Biblia Takatifu

Tafsiri ya Ulimwengu Mpya

ITALIA
ROMA
MAKEDONIA
Filipi
UGIRIKI
ATHENE
Korintho
Efeso
SISILI
PATMO
RODE
MALTA
KRETE
Bahari ya Mediterania
(Bahari Kuu)
LIBYA
Kask.
0 maili
500
0 km
500

Bahari Nyeusi
MIL. ARARATI
ASIA NDOGO
Bustani ya Edeni?
Antiokia (ya Pisidia)
ASHURU
UMEDI
Tarso
Harani
Antiokia (ya Siria)
NINAWI
KIPRO
SIRIA
Mto Efrati
Mto Tigri
Sidoni
Damasko
Tiro
Kaisaria
NCHI YA AHADI
YERUSALEMU
BABILONI
Shushani
MOABU
UKALDAYO
Kadeshi
Uru
MEMFISI
EDOMU
MISRI
Ml. Sinai
ARABIA
Mto Nile
Bahari Nyekundu
bi12-SW

Biblia Takatifu
Tafsiri ya Ulimwengu Mpya

Biblia hii imetafsiriwa kutoka chapa ya Kiingereza
ya *New World Translation of the Holy Scriptures,*
iliyorekebishwa 1984

"Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova [יהוה, *YHWH*] amesema hivi:
' . . . Mimi ninaumba mbingu mpya na dunia mpya;
na mambo ya zamani hayatakumbukwa akilini,
wala hayataingia moyoni.'"
—Isaya 65:13, 17; ona pia 2 Petro 3:13.

© 2003
WATCH TOWER BIBLE AND TRACT SOCIETY
OF PENNSYLVANIA
ASSOCIAÇÃO TORRE DE VIGIA DE BÍBLIAS E TRATADOS

Biblia Takatifu—Tafsiri ya Ulimwengu Mpya

WACHAPISHAJI
WATCHTOWER BIBLE AND TRACT SOCIETY
OF NEW YORK, INC.
Brooklyn, New York, U.S.A.
ASSOCIAÇÃO TORRE DE VIGIA DE BÍBLIAS E TRATADOS
Rodovia SP-141, km 43, Cesário Lange, SP, 18285-901, Brasil

Biblia hii imechapishwa ikiwa nzima katika Kiafrikana, Kialbania, Kiarabu, Kiarmenia, Kibemba, Kibulgaria, Kicheki, Kichewa, Kichina (cha Kitamaduni), Kichina (Kilicho Rahisi), Kidachi, Kidenishi, Kiefik, Kifaransa, Kifini, Kigeorgia, Kigiriki, Kihispania (pia katika Maandishi ya Vipofu), Kihosa, Kihungaria, Kiigbo, Kiiloko, Kiindonesia, Kiingereza (pia katika Maandishi ya Vipofu), Kiitaliano, Kijapani, Kijerumani, Kikirghiz, Kikorea, Kikroatia, Kilingala, Kimakedonia, Kimalagasi, Kimalta, Kinorwei, Kinyarwanda, Kiosetia, Kipolishi, Kireno (pia katika Maandishi ya Vipofu), Kirumania, Kirundi, Kirusi, Kisamoa, Kisebuano, Kisepedi, Kiserbia, Kiserbia (cha Kiroma), Kisesotho, Kishona, Kisinhala, Kislovaki, Kislovenia, Kisranantongo, Kiswahili, Kiswedi, Kitagalogi, Kitsonga, Kitswana, Kituruki, Kitwi (cha Akuapem), Kitwi (cha Asante), Kiyoruba, na Kizulu

(Pia Biblia hii imechapishwa ikiwa sehemu katika Kiamhara, Kiazerbaijani, Kiazerbaijani [cha Kisirili], Kiestonia, Kiewe, Kifiji, Kiganda, Kiguni, Kihiligaynoni, Kihindi, Kihiri Motu, Kiitaliano cha Maandishi ya Vipofu, Kikambodia, Kikanada, Kikaonde, Kikazakh, Kikiribati, Kikreoli cha Haiti, Kilatvia, Kilithuania, Kiluvale, Kimalayalam, Kimaya, Kimyanmar, Kinepali, Kipangasinani, Kipapiamento (cha Kurasao), Kipijini cha Visiwa vya Solomon, Kipunjabi, Kisango, Kisilozi, Kitamili, Kitartar, Kitetum, Kithai, Kitigrinya, Kitok Pisin, Kitonga, Kitumbuka, Kituvalu, Kiukrania, Kiuzbek, Kivenda, Kivietnam, Kiwaray-Waray, Lugha ya Ishara ya Brazili [katika DVD], Lugha ya Ishara ya Italia [katika DVD], Lugha ya Ishara ya Kolombia [katika DVD], Lugha ya Ishara ya Marekani [katika DVD], Lugha ya Ishara ya Mexico [katika DVD], na Lugha ya Ishara ya Urusi [katika DVD]

Nakala 208,366,928 za Chapa Zote za
Tafsiri ya Ulimwengu Mpya zimechapwa

Chapa ya 2006
Biblia hii haiuzwi. Ni sehemu ya kazi ya elimu ya Biblia
ya ulimwenguni pote ya Mashahidi wa Yehova.

New World Translation of the Holy Scriptures
Swahili (*bi12*-SW)

Made in Brazil Imechapishwa Brazil

UTANGULIZI

BIBLIA TAKATIFU ni ufunuo kutoka kwa Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova ulioandikiwa watu wote katika dunia hii. Kitabu hiki kilichoongozwa na roho ya Mungu kinavutia watu duniani kote, kwa kuwa kina habari njema za Ufalme wa Mungu, ambao utasimamisha amani na uadilifu. Dunia itakuwa paradiso kwa ajili ya watu wote. Biblia inaonyesha kwamba kwa upendo Mungu aliandaa wokovu kutoka kwenye kifo kwa ajili ya ulimwengu wa wanadamu wenye dhambi, naye alifanya hivyo kupitia dhabihu ya fidia ya Mwana wake, Yesu Kristo.—Yohana 3:16.

Mwanzoni Biblia iliandikwa katika Kiebrania, Kiaramu (lugha yenye uhusiano na Kiebrania), na Kigiriki. Kwa kuwa ni watu wachache leo ambao wanaelewa lugha hizo, imekuwa lazima Biblia Takatifu itafsiriwe katika lugha za kisasa ili kuutangaza ujumbe wake unaotokeza uzima kwa watu wa mataifa yote.

Tafsiri hii mpya ya Biblia ya Kiswahili inategemea chapa ya Kiingereza ya *New World Translation of the Holy Scriptures* ya mwaka wa 1984. Ina vitabu 39 vya Maandiko ya Kiebrania na Kiaramu na tafsiri iliyorekebishwa ya Kiswahili ya vitabu 27 vya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo iliyochapishwa 1996. Halmashauri ya Kutafsiri Biblia ya Ulimwengu Mpya iliamua sehemu hizo mbili za Maandiko Matakatifu ziitwe kwa majina ya lugha za kwanza ambazo zilitumiwa kuandika sehemu hizo badala ya kutumia majina yanayotumiwa kwa ukawaida "Agano la Kale" na "Agano Jipya." Hiyo ni kwa sababu kwa kweli Biblia ni kitabu kimoja tu, na hakuna sehemu iliyopitwa na wakati, au kuwa ya "kale." Ujumbe wake unapatana kuanzia kitabu cha kwanza cha sehemu ya Kiebrania mpaka kitabu cha mwisho cha sehemu ya Kigiriki. Ili kumsaidia msomaji katika funzo lake la Biblia nzima, tumetia ndani marejeo zaidi ya 125,000 na fahirisi ya baadhi ya maneno ya Biblia.

Kwa kuwa Biblia hueleza mapenzi matakatifu ya Bwana Mwenye Enzi Kuu ya ulimwengu wote, kuliondoa au kulificha jina la pekee la Mungu, ambalo linapatikana waziwazi mara 7,000 hivi katika maandishi ya Kiebrania, ni ukosefu mkubwa wa heshima, na jambo hilo kwa kweli ni kuukaidi utukufu na mamlaka yake. Kwa hiyo, jambo linalotokeza zaidi katika tafsiri hii ni kule kulirudisha jina la Mungu mahali pake panapofaa katika maandishi ya Biblia. Jambo hilo limefanywa kwa kutumia jina "Yehova" ambalo linakubalika na wengi katika Kiswahili, mara 6,973 katika Maandiko ya Kiebrania na mara 237 katika Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo. Ili kupata habari zaidi kuhusu jina hilo, tazama sehemu ya Nyongeza ya tafsiri hii.

Watafsiri wa kitabu hiki, ambao wanampenda Mungu aliye Mtungaji wa Maandiko Matakatifu, wanatambua kwamba wana wajibu wa pekee kwake wa kupitisha mawazo na matangazo yake kwa usahihi kadiri inavyowezekana. Wanatambua pia kwamba wana wajibu kwa wasomaji wanaofanya uchunguzi, ambao wanaitegemea tafsiri ya Neno lililoongozwa na roho ya Mungu Aliye Juu Zaidi kwa ajili ya wokovu wao wa milele. Tunatumaini kwa unyoofu kwamba kwa msaada wa tafsiri hii, msomaji ataweza kuipata njia inayoongoza kwenye uzima usio na mwisho katika ulimwengu mpya wenye uadilifu wa Mweza-Yote.—Isaya 65:17; 2 Petro 3:13.

—*Wachapishaji*

MAJINA NA UTARATIBU WA VITABU:
vya Maandiko ya Kiebrania na Kiaramu

Kitabu	Ufupisho	Uku.
Mwanzo	Mwa	7
Kutoka	Kut	90
Mambo ya Walawi	Law	158
Hesabu	Hes	208
Kumbukumbu la Torati	Kum	277
Yoshua	Yos	336
Waamuzi	Amu	374
Ruthu	Ru	415
1 Samweli	1Sa	420
2 Samweli	2Sa	472
1 Wafalme	1Fa	517
2 Wafalme	2Fa	569
1 Mambo ya Nyakati	1Nya	618
2 Mambo ya Nyakati	2Nya	663
Ezra	Ezr	718
Nehemia	Ne	733
Esta	Est	756
Ayubu	Ayu	769
Zaburi	Zb	826
Methali	Met	976
Mhubiri	Mhu	1015
Wimbo wa Sulemani	Wim	1028
Isaya	Isa	1035
Yeremia	Yer	1123
Maombolezo	Omb	1219
Ezekieli	Eze	1231
Danieli	Da	1322
Hosea	Ho	1349
Yoeli	Yoe	1362
Amosi	Amo	1366
Obadia	Oba	1376
Yona	Yon	1378
Mika	Mik	1381
Nahumu	Nah	1389
Habakuki	Hab	1392
Sefania	Sef	1396
Hagai	Hag	1400
Zekaria	Zek	1402
Malaki	Mal	1417

vya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo

Kitabu	Ufupisho	Uku.
Mathayo	Mt	1422
Marko	Mk	1475
Luka	Lu	1508
Yohana	Yoh	1566
Matendo	Mdo	1609
Waroma	Ro	1664
1 Wakorintho	1Ko	1686
2 Wakorintho	2Ko	1707
Wagalatia	Gal	1722
Waefeso	Efe	1729
Wafilipi	Flp	1737
Wakolosai	Kol	1743
1 Wathesalonike	1Th	1748
2 Wathesalonike	2Th	1753
1 Timotheo	1Ti	1755
2 Timotheo	2Ti	1762
Tito	Tit	1766
Filemoni	Flm	1769
Waebrania	Ebr	1770
Yakobo	Yak	1787
1 Petro	1Pe	1793
2 Petro	2Pe	1799
1 Yohana	1Yo	1803
2 Yohana	2Yo	1809
3 Yohana	3Yo	1810
Yuda	Yud	1811
Ufunuo	Ufu	1813

MWANZO

1 Hapo mwanzo[a] Mungu[b] aliumba[c] mbingu na dunia.[d]
2 Dunia ilikuwa bila umbo,
na ukiwa, na giza lilikuwa juu
ya uso wa kilindi cha maji;[e] na
nguvu za utendaji za Mungu zilikuwa zikienda huku na huku[f]
juu ya uso wa maji.[g]
3 Mungu akasema:[h] "Kuwe
na nuru." Kukawa na nuru.[i]
4 Kisha Mungu akaona ya
kuwa nuru ilikuwa nzuri. Mungu akateganisha nuru na
giza.[j] **5** Mungu akaanza kuiita nuru Mchana,[k] lakini giza
akaliita Usiku.[l] Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya kwanza.
6 Mungu akaendelea kusema: "Kuwe na anga[m] kati ya
hayo maji na mtengano uwepo
kati ya maji na maji."[n] **7** Ndipo Mungu akalifanya anga na
kutenganisha maji yaliyo chini
ya anga na maji yaliyo juu
ya anga.[o] Ikawa hivyo. **8** Mungu akaanza kuliita anga, Mbingu.[p] Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya pili.
9 Mungu akaendelea kusema: "Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, nayo nchi kavu ionekane."[q] Ikawa hivyo. **10** Na Mungu akaanza kuiita hiyo nchi
kavu Dunia,[r] lakini mkusanyiko wa maji akauita Bahari.[s] Kisha Mungu akaona ya kuwa
ilikuwa vyema.[t] **11** Mungu
akaendelea kusema: "Dunia
na itoe majani, mimea inayozaa mbegu,[u] miti ya matunda
inayozaa matunda kulingana
na aina zake,[v] ambayo mbegu
yake imo ndani yake,[w] juu ya
nchi." Ikawa hivyo. **12** Nayo
dunia ikaanza kutokeza majani, mimea inayozaa mbegu
kulingana na aina yake[a] na
miti inayozaa matunda, ambayo mbegu yake imo ndani yake
kulingana na aina yake.[b] Kisha Mungu akaona ya kuwa ilikuwa vyema. **13** Ikawa jioni,
ikawa asubuhi, siku ya tatu.
14 Mungu akaendelea kusema: "Kuwe na mianga katika anga la mbingu ili kutenganisha mchana na usiku;[c] nayo
iwe ishara na kwa ajili ya majira na kwa ajili ya siku na miaka.[d] **15** Nayo iwe mianga katika anga la mbingu ili iangaze
dunia."[e] Ikawa hivyo. **16** Na
Mungu akaifanya mianga mikubwa miwili. Mwanga mkubwa utawale mchana na mwanga mdogo utawale usiku, na
pia nyota.[f] **17** Basi Mungu
akaiweka katika anga la mbingu ili iangaze dunia,[g] **18** na
kutawala mchana na usiku na
kutenganisha nuru na giza.[h]
Kisha Mungu akaona ya kuwa
ilikuwa vyema.[i] **19** Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya nne.
20 Mungu akaendelea kusema: "Maji na yajawe na nafsi hai[j] na viumbe vinavyoruka viruke juu ya dunia kwenye uso
wa anga la mbingu."[k] **21** Mungu akaanza kuumba wanyama wakubwa mno wa baharini[l]
na kila nafsi hai inayotembea,[m]
wakajaa majini kulingana na
aina zake, na kila kiumbe kinachoruka chenye mabawa kulingana na aina yake.[n] Kisha

SURA 1

a Ebr 1:10
b Kut 6:3
Kut 33:20
Kum 6:4
Mk 10:18
Yoh 4:24
Ro 1:20
1Ko 8:4
1Ti 1:11
1Ti 2:5
Ebr 9:24
1Yo 4:16
Ufu 4:8
c Zb 148:5
Isa 45:18
Ufu 4:11
d Ayu 38:4
Zb 102:25
Isa 42:5
Ufu 10:6
e Ayu 38:30
Met 8:27
f Zb 33:6
Isa 40:26
g Zb 104:6
h Zb 33:9
i Isa 45:7
j Ayu 26:10
2Ko 4:6
k Mwa 8:22
l Yer 33:20
m Mwa 1:20
n Zb 33:7
2Pe 3:5
o Mwa 7:11
Met 8:28
p Mwa 27:28
Kum 4:17
1Fa 8:35
q Ayu 38:11
Zb 104:8
Zb 136:6
r Zb 24:1
Zb 95:5
s Ayu 38:8
Met 8:29
t Kum 32:4
1Ti 4:4
u Mwa 1:29
Zb 72:16
Mt 13:32
v Lu 6:44
w Hag 2:19
Yak 3:12

Safu ya 2

a Law 19:19
Zb 104:14
b Ga 6:7
c Kum 4:19
Zb 148:3
d Mwa 8:22
1Nya 23:31
Zb 104:19
e Yer 33:25
Eze 32:8
f Zb 8:3
Zb 136:8
Yer 31:35
g Isa 13:10
h Zb 74:16
Isa 45:7
i Zb 104:31
j Law 11:10
k Mwa 2:19
Mwa 9:10
Kum 4:17
Ayu 12:7

l Ayu 7:12; Zb 148:7; m Law 11:46; n Mwa 7:14; Law 11:14; Kum 14:13; 1Ko 15:39.

Mungu akaona ya kuwa ilikuwa vyema. **22** Halafu Mungu akawabariki, akisema: "Zaeni, muwe wengi na kujaza maji yaliyo katika mabonde ya bahari,[a] na viumbe vinavyoruka na viwe vingi duniani." **23** Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya tano.

24 Mungu akaendelea kusema: "Dunia[b] na itokeze nafsi zilizo hai kulingana na aina zake, mnyama wa kufugwa[c] na mnyama anayetambaa[d] na mnyama-mwitu[e] wa dunia kulingana na aina yake." Ikawa hivyo. **25** Mungu akafanya mnyama-mwitu wa dunia kulingana na aina yake na mnyama wa kufugwa kulingana na aina yake na kila mnyama anayetembea wa nchi kulingana na aina yake.[f] Mungu akaona ya kuwa ilikuwa vyema.

26 Mungu akaendelea kusema: "Na tufanye[g] mtu kwa mfano[h] wetu, kwa sura[i] yetu, nao watawale samaki wa baharini na viumbe vinavyoruka vya mbinguni na wanyama wa kufugwa na dunia yote na kila mnyama anayetembea juu ya dunia."[j] **27** Mungu akamuumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba;[k] mwanamume na mwanamke aliwaumba.[l] **28** Mungu akawabariki[m] na Mungu akawaambia: "Zaeni,[n] muwe wengi, mjaze dunia na kuitiisha,[o] na mtawale[p] samaki wa baharini na viumbe vinavyoruka vya mbinguni na kila kiumbe hai kinachotambaa juu ya dunia."

29 Mungu akaendelea kusema: "Tazama nimewapa mimea yote inayozaa mbegu iliyo juu ya uso wa dunia yote na kila mti ambao una matunda ya mti unaozaa mbegu.[a] Na iwe chakula kwenu.[b] **30** Na mimea yote ya majani nimetoa iwe chakula[c] kwa kila mnyama-mwitu wa dunia na kila kiumbe kinachoruka cha mbinguni na kila kitu kinachotembea juu ya dunia ambacho ndani yake mna uhai ukiwa nafsi." Ikawa hivyo.

31 Kisha Mungu akaona kila kitu alichokuwa amefanya na, tazama! kilikuwa chema sana.[d] Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya sita.

2 Basi mbingu na dunia na jeshi lake lote zikamalizika.[e] **2** Na kufikia siku ya saba Mungu akamaliza kazi yake ambayo alikuwa ameifanya, naye akaanza kupumzika siku ya saba kutokana na kazi yake yote ambayo alikuwa ameifanya.[f] **3** Mungu akaibariki siku ya saba na kuifanya takatifu, kwa kuwa katika siku hiyo amekuwa akipumzika kutokana na kazi yake yote ya kuumba ambayo Mungu alikusudia kuifanya.[g]

4 Hii ndiyo historia ya mbingu na dunia wakati zilipoumbwa, katika siku ambayo Yehova Mungu aliifanya dunia na mbingu.[h]

5 Basi, mti wa shambani haukuwapo duniani wala mimea ya shambani ilikuwa haijachipuka bado, kwa kuwa Yehova Mungu hakuwa amenyesha mvua[i] juu ya dunia wala hapakuwa na mtu wa kuilima nchi. **6** Lakini ukungu[j] ulikuwa ukipanda kutoka katika dunia na kuunywesha maji uso wote wa nchi.[k]

7 Na Yehova Mungu akamfanya mtu kutoka katika ma-

SURA 1

a Ne 9:6
Zb 104:25
b Mhu 3:20
c Kum 28:11
Ufu 10:6
d Mwa 6:7
e Zb 104:11
Mk 1:13
f Mwa 7:14
Zb 148:10
g Mwa 11:7
Met 8:30
Yoh 1:3
Kol 1:16
h Mwa 9:6
1Ko 11:7
Kol 3:10
i Mwa 5:1
Mdo 17:29
Yak 3:9
j Mwa 9:2
k Zb 139:14
l Mk 10:6
1Ko 11:9
m Zb 107:38
n Mwa 9:1
Law 26:9
o Mwa 2:15
p Zb 8:6
Isa 11:9
Yak 3:7

Safu ya 2

a Ayu 36:31
Zb 145:16
b Mwa 9:3
Zb 104:14
Mdo 14:17
c Zb 136:25
Zb 147:9
Mt 6:26
d Kum 32:4
Zb 104:24
1Ti 4:4

SURA 2

e Ne 9:6
Zb 146:6
Isa 42:5
Zek 12:1
Mdo 4:24
f Kut 31:17
Ebr 4:4
g Kut 20:11
h Isa 45:18
i Mt 5:45
j Ayu 36:27
k Zb 135:7

vumbi[a] ya nchi[b] na kupuliza katika mianzi ya pua yake pumzi ya uhai,[c] naye mtu akawa nafsi hai.[d] **8** Na Yehova Mungu akapanda bustani katika Edeni,[e] kuelekea mashariki, na hapo akamweka mtu ambaye alikuwa amemfanya.[f] **9** Hivyo Yehova Mungu akachipusha katika nchi kila mti wenye kutamanika kwa macho ya mtu na ulio mwema kwa ajili ya chakula na pia mti wa uzima[g] katikati ya bustani na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.[h]

10 Kulikuwa na mto unaotoka katika Edeni ili kuinywesha bustani maji, na kutoka hapo ukaanza kugawanyika na kuwa vichwa vinne. **11** Jina la ule wa kwanza ni Pishoni; ndio unaozunguka nchi yote ya Havila,[i] ambako kuna dhahabu. **12** Nayo dhahabu ya nchi hiyo ni nzuri.[j] Pia kuna ulimbo wa bedola[k] na jiwe la shohamu.[l] **13** Na jina la mto wa pili ni Gihoni; ndio unaozunguka nchi yote ya Kushi. **14** Na jina la mto wa tatu ni Hidekeli;[m] ndio unaoelekea upande wa mashariki wa Ashuru.[n] Na mto wa nne ni Efrati.[o]

15 Na Yehova Mungu akamchukua mtu na kumweka katika bustani ya Edeni,[p] ailime na kuitunza.[q] **16** Pia Yehova Mungu akamwekea mtu amri hii: "Matunda ya kila mti wa bustani unaweza kula mpaka ushibe.[r] **17** Lakini kuhusu matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula, utakufa hakika."[s]

18 Na Yehova Mungu akaendelea kusema: "Si vema huyo mwanamume aendelee kuwa peke yake. Nitamfanyia msaidizi, awe kikamilisho chake."[a] **19** Yehova Mungu alikuwa akifanya kutoka katika udongo kila mnyama wa mwituni na kila kiumbe kinachoruka cha mbinguni, naye akaanza kumletea huyo mtu ili aone atawaitaje kila mmoja wao; na jina ambalo huyo mtu aliita kila nafsi hai,[b] kila mmoja, hilo likawa jina lake.[c] **20** Basi huyo mtu alikuwa akiita majina wanyama wote wa kufugwa na viumbe vinavyoruka vya mbinguni na kila mnyama wa mwituni, lakini kwa ajili ya huyo mwanamume hakupatikana msaidizi wa kuwa kikamilisho chake. **21** Kwa hiyo Yehova Mungu akamletea huyo mwanamume usingizi mzito,[d] na alipokuwa akilala, akachukua ubavu wake mmoja na kisha akafunika nyama mahali pake. **22** Na Yehova Mungu akaufanya ubavu ambao alikuwa ameuchukua kutoka kwa mwanamume kuwa mwanamke na kumleta kwa huyo mwanamume.[e]

23 Ndipo huyo mwanamume akasema:

"Mwishowe huyu ni mfupa
wa mifupa yangu
Na nyama ya nyama
yangu.[f]
Huyu ataitwa Mwanamke,
Kwa sababu huyu
alitolewa katika
mwanamume."[g]

24 Hiyo ndiyo sababu mwanamume atamwacha baba yake na mama yake[h] naye atashikamana na mke wake nao watakuwa mwili mmoja.[i] **25** Na wote wawili walikuwa uchi,[j] huyo mwanamume na mke wake, lakini hawakuona haya.[k]

SURA 2

a Mwa 3:19
Zb 103:14
Mhu 3:20
1Ko 15:47
b Ayu 33:6
Isa 64:8
c Mwa 7:22
Ayu 27:3
Ayu 33:4
Isa 42:5
Mdo 17:25
d Eze 18:4
1Ko 15:45
1Pe 3:20
e Mwa 2:15
Mwa 3:23
Isa 51:3
Eze 28:13
f Mwa 1:26
Zb 139:14
Ro 9:20
g Mwa 3:24
h Mwa 2:17
Mwa 3:22
i Mwa 25:18
1Sa 15:7
j Mwa 13:2
k Hes 11:7
l Kut 25:7
1Nya 29:2
Ayu 28:16
m Da 10:4
n Mwa 10:11
Mik 5:6
o Mwa 15:18
Kum 11:24
p Mwa 3:24
Eze 28:13
q Mwa 1:28
Mwa 2:8
Zb 115:16
r Mwa 2:9
Mwa 3:2
Law 25:19
s Mwa 3:19
Zb 146:4
Mhu 9:5
Eze 18:4
Ro 5:12
1Ko 15:22

Safu ya 2

a Met 31:11
1Ko 11:9
1Ti 2:13
b Mwa 9:10
c Mwa 1:26
Mwa 9:2
Zb 8:6
d 1Sa 26:12
e Met 18:22
Met 19:14
Mk 10:9
1Ti 2:13
f Mwa 29:14
Amu 9:2
2Sa 5:1
2Sa 19:12
g 1Ko 11:8
h Mwa 24:58
Zb 45:10
Mk 10:7
i Met 5:18
Mal 2:16
Mt 19:5
Ro 7:2
1Ko 6:16
1Ko 7:10
Efe 5:31
Ebr 13:4
j Mwa 3:7
k Zb 31:17

3 Basi nyoka[a] alikuwa mwenye kujihadhari[b] kuliko wanyama wote wa mwituni ambao Yehova Mungu alikuwa amewafanya.[c] Kwa hiyo akaanza kumwambia mwanamke:[d] "Je, ni kweli kwamba Mungu alisema msile matunda ya kila mti wa bustani?"[e] **2** Mwanamke akamjibu na kumwambia nyoka: "Tunaweza kula matunda ya miti ya bustani.[f] **3** Lakini kuhusu kula matunda ya mti ulio katikati ya bustani,[g] Mungu amesema, 'Msiyale, wala msiyaguse ili msife.'"[h] **4** Ndipo nyoka akamwambia mwanamke: "Hakika hamtakufa.[i] **5** Kwa maana Mungu anajua kwamba siku ileile mtakapokula matunda yake macho yenu yatafunguliwa, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya."[j]

6 Basi mwanamke akaona kwamba mti huo ulikuwa mzuri kwa chakula na kwamba ulikuwa kitu cha kutamanika kwa macho, ndiyo, mti huo ulikuwa wenye kupendeza kuutazama.[k] Kwa hiyo akaanza kuchukua kati ya matunda yake akala. Baadaye akampa mume wake pia alipokuwa pamoja naye, naye akaanza kula.[l] **7** Ndipo macho yao wote wawili yakafunguliwa nao wakaanza kutambua kwamba walikuwa uchi.[m] Kwa hiyo wakashona majani ya mtini ya kujifunika kiunoni.[n]

8 Baadaye wakasikia sauti ya Yehova Mungu akitembea katika bustani karibu na wakati wenye upepo mtulivu wa siku,[o] naye huyo mwanamume na mke wake wakajificha kutoka mbele za uso wa Yehova Mungu katikati ya miti ya bustani.[p]

SURA 3

a 2Ko 11:3
Ufu 12:9
Ufu 20:2
b Mt 10:16
c Mwa 1:24
d Mwa 2:22
Hes 22:28
e Mwa 2:17
f Mwa 2:16
g Mwa 2:9
h Kut 19:12
i Mwa 5:5
Yoh 8:44
1Yo 3:8
Ufu 21:8
j Mwa 3:22
Isa 46:5
Flp 2:6
k Yak 1:14
1Yo 2:16
l Ro 5:12
2Ko 11:3
1Ti 2:14
m Ayu 1:21
n Mwa 3:21
o Kum 4:33
Kum 23:14
Mdo 7:31
p Da 10:7
Amo 9:3
Ebr 4:13
1Yo 4:18

Safu ya 2

a Mik 6:9
b Kut 3:6
c Mwa 2:25
d Mwa 2:17
e 1Sa 15:24
Yak 1:14
f 2Ko 11:3
1Ti 2:14
g Mwa 3:1
h Isa 65:25
Mik 7:17
i Isa 35:4
Isa 43:11
Ebr 10:31
j Mwa 22:17
Yak 4:4
Yud 9
Ufu 12:7
Ufu 12:17
k Eze 28:14
Ufu 12:9
l Isa 54:5
Ga 4:26
Ufu 12:1
m Mt 23:33
Yoh 8:44
1Yo 3:10
n Mwa 22:18
Mwa 49:10
Ga 3:16
Ga 3:29
o Yoh 18:37
p Ufu 20:2
q Ufu 20:10
r Ebr 2:14
s Mik 5:1
Mt 27:50
t Mdo 3:15
Flp 2:8
u 1Nya 4:9
v Mwa 35:16
w 1Ko 7:28
x Mwa 2:17
Mhu 12:13
y Mwa 4:12
Mwa 5:29

9 Na Yehova Mungu akaendelea kumwita huyo mwanamume na kumuuliza: "Uko wapi?"[a] **10** Mwishowe akasema: "Niliisikia sauti yako katika bustani, lakini niliogopa kwa sababu nilikuwa uchi, na basi nikajificha."[b] **11** Ndipo akasema: "Ni nani alikuambia ya kwamba ulikuwa uchi?[c] Je, umekula matunda ya mti ambao nilikuamuru usile matunda yake?"[d] **12** Na huyo mwanamume akaendelea kusema: "Mwanamke uliyenipa awe pamoja nami, alinipa tunda kutoka katika ule mti nami nikala."[e] **13** Kwa hiyo Yehova Mungu akamwambia mwanamke: "Ni nini hili ulilofanya?" Mwanamke akajibu: "Yule nyoka—alinidanganya nami nikala."[f]

14 Na Yehova Mungu akamwambia nyoka:[g] "Kwa sababu umefanya jambo hili, umelaaniwa kati ya wanyama wote wa kufugwa na kati ya wanyama wote wa mwituni. Utakwenda kwa tumbo lako na utakula mavumbi siku zote za maisha yako.[h] **15** Nami[i] nitaweka uadui[j] kati yako[k] na yule mwanamke[l] na kati ya uzao wako[m] na uzao wake.[n] Yeye[o] atakuponda[p] kichwa[q] nawe[r] utamtia jeraha[s] kwenye kisigino."[t]

16 Akamwambia mwanamke: "Nitazidisha sana maumivu ya mimba yako;[u] kwa uchungu utazaa watoto,[v] na tamaa yako itakuwa kwa mume wako, naye atakutawala."[w]

17 Naye akamwambia Adamu: "Kwa sababu uliisikiliza sauti ya mke wako ukala matunda ya mti ambao nilikupa amri[x] hii kuuhusu, 'Usile matunda yake,' udongo umelaaniwa kwa sababu yako.[y] Kwa mau-

mivu utakula mazao yake siku
zote za maisha yako.[a] **18** Nao
utakuzalia miiba na mibaru-
ti,[b] nawe utakula mimea ya
shambani. **19** Kwa jasho la
uso wako utakula mkate mpa-
ka utakaporudi katika udo-
ngo, kwa kuwa ulitolewa kati-
ka huo.[c] Kwa maana wewe ni
mavumbi nawe utarudi mavu-
mbini."[d]

20 Baada ya hayo Adamu
akamwita mke wake jina lake
Hawa,[e] kwa sababu ndiye ange-
kuja kuwa mama ya kila mtu
anayeishi.[f] **21** Na Yehova Mu-
ngu akawafanyia Adamu na
mke wake mavazi marefu ya
ngozi, akawavika.[g] **22** Na Ye-
hova Mungu akaendelea kuse-
ma: "Tazama, huyu mtu ame-
kuwa kama mmoja wetu kwa
kujua mema na mabaya,[h] na
sasa ili asije akanyoosha mko-
no wake achukue matunda ku-
toka pia katika mti wa uzima[i]
na kula na kuishi mpaka waka-
ti usio na kipimo,—" **23** Kwa
hiyo Yehova Mungu akamwo-
ndoa katika bustani ya Edeni[j]
ili aulime udongo ambao
katika huo alikuwa ametole-
wa.[k] **24** Na basi akamfukuza
huyo mtu, akaweka upande wa
mashariki wa bustani ya Edeni[l]
makerubi[m] na upanga unaowa-
ka ambao ulikuwa unajizungu-
sha-zungusha ili kuilinda njia
ya kwenda kwenye ule mti wa
uzima.

4 Basi Adamu akalala na
Hawa mke wake naye aka-
pata mimba.[n] Baada ya muda
akamzaa Kaini[o] na kusema:
"Nimezaa mwanamume kwa
msaada wa Yehova."[p] **2** Baa-
daye akazaa tena, Abeli[q] ndugu
yake.

SURA 3
a Zb 127:2
Hag 1:6
b Ebr 6:8
c Mwa 2:7
d Ayu 34:15
Mhu 3:20
e Mwa 2:19
Mwa 4:1
f Mdo 17:26
g Mwa 3:7
Ufu 3:18
h Mwa 3:5
Flp 2:6
i Mwa 2:9
j Mwa 2:8
k Mwa 2:5
Mwa 3:19
l Mwa 2:8
Mwa 4:16
m Zb 80:1
Isa 37:16
Eze 10:4

SURA 4
n Mwa 1:28
o Yud 11
p Mwa 3:16
q Mt 23:35

Safu ya 2
a Mwa 46:34
b Mwa 3:23
c Ne 10:35
d Law 2:14
e Kut 13:12
f Law 3:9
g Ebr 11:4
h Amo 5:22
i Met 14:30
Met 15:18
Met 27:4
j Lu 14:11
1Pe 5:6
k Met 11:6
Yak 1:14
l Mhu 8:13
Eze 18:27
m Mt 23:35
1Yo 3:12
Yud 11
n Zb 10:13
Met 28:13
o Zb 50:20
Met 17:17
p Mwa 18:20
2Fa 9:26
Isa 26:21
Ebr 12:24
q Ezr 7:26
r Mwa 9:5
s Mwa 3:17
Law 26:20
Kum 28:18

Naye Abeli akawa mchunga-
ji wa kondoo,[a] bali Kaini akawa
mkulima wa udongo.[b] **3** Ika-
wa kwamba baada ya wakati fu-
lani kwisha Kaini akaleta ma-
zao ya udongo[c] yawe toleo kwa
Yehova.[d] **4** Abeli naye akale-
ta baadhi ya wazaliwa wa kwa-
nza[e] wa kundi lake, pia vipande
vyao vyenye mafuta.[f] Ingawa
Yehova alikuwa akimtazama
Abeli na toleo lake kwa kibali,[g]
5 hakumtazama Kaini na to-
leo lake kwa kibali chocho-
te.[h] Ndipo Kaini akawaka ha-
sira,[i] na uso wake ukaanza ku-
kunjamana. **6** Basi Yehova
akamwambia Kaini: "Kwa
nini umewaka hasira na kwa
nini uso wako umekunjamana?
7 Ukigeuka utende mema, je,
hutainuliwa?[j] Lakini usipogeu-
ka utende mema, kuna dha-
mbi inayovizia katika mwingi-
lio, nayo inakutamani[k] wewe.
Je, wewe utaishinda?"[l]

8 Baada ya hayo Kaini aka-
mwambia Abeli ndugu yake:
"Twende shambani." Basi ika-
wa kwamba walipokuwa sha-
mbani Kaini akamshambulia
Abeli ndugu yake, akamuua.[m]
9 Baadaye Yehova akamuuliza
Kaini: "Yuko wapi Abeli ndu-
gu yako?"[n] naye akasema: "Si-
jui. Kwani mimi ni mlinzi wa
ndugu yangu?"[o] **10** Kwa hiyo
akasema: "Umefanya nini? Si-
kiliza! Damu ya ndugu yako
inanililia kutoka katika udo-
ngo.[p] **11** Na sasa umelaani-
wa kwa kufukuzwa kutoka
katika udongo,[q] ambao umefu-
ngua kinywa chake ili ku-
pokea damu ya ndugu yako
kwa mkono wako.[r] **12** Uta-
kapoulima udongo, hautaku-
rudishia nguvu zake.[s] Utaku-
wa mwenye kutanga-tanga na

mkimbizi duniani."[a] **13** Kwa hiyo Kaini akamwambia Yehova: "Adhabu yangu ya kosa ni kubwa mno, haichukuliki. **14** Tazama unanifukuza leo kutoka usoni pa udongo, nami nitafichwa kutoka usoni pako;[b] nami nitakuwa mwenye kutanga-tanga[c] na mkimbizi duniani, na itakuwa kwamba yeyote atakayenikuta ataniua."[d] **15** Ndipo Yehova akamwambia: "Kwa sababu hiyo yeyote anayemuua Kaini atalipizwa kisasi mara saba."[e]

Hivyo Yehova akaweka ishara kwa ajili ya Kaini ili kwamba yeyote anayemkuta asimpige.[f] **16** Ndipo Kaini akaenda zake kutoka usoni pa Yehova[g] na kukaa katika nchi ya Ukimbizi upande wa mashariki wa Edeni.

17 Baadaye Kaini akalala na mke wake[h] naye akapata mimba, akamzaa Enoko. Kisha akajishughulisha na ujenzi wa jiji, akaliita hilo jiji kwa jina la mwana wake Enoko.[i] **18** Baadaye Enoko akazaa mwana anayeitwa Iradi. Na Iradi akamzaa Mehuyaeli, na Mehuyaeli akamzaa Methushaeli, na Methushaeli akamzaa Lameki.

19 Na Lameki akajichukulia wake wawili. Jina la wa kwanza lilikuwa Ada na jina la wa pili lilikuwa Zila. **20** Baada ya muda Ada akamzaa Yabali. Akawa mwanzilishi wa wale wanaokaa katika mahema[j] na walio na mifugo.[k] **21** Na jina la ndugu yake lilikuwa Yubali. Akawa mwanzilishi wa wote wanaotumia kinubi[l] na zumari.[m] **22** Zila naye pia akamzaa Tubal-kaini, mfuaji wa kila namna ya vifaa vya shaba na chuma.[a] Na dada yake Tubal-kaini alikuwa Naama. **23** Basi Lameki akatunga maneno haya kwa ajili ya wake zake Ada na Zila:

"Sikieni sauti yangu, enyi wake za Lameki;
Tegeni sikio kwa maneno yangu:
Nimemuua mtu kwa kunitia jeraha,
Naam, kijana kwa kunipiga.
24 Ikiwa Kaini atalipizwa kisasi mara 7,[b]
Basi Lameki ni mara 77."

25 Naye Adamu akalala na mke wake tena naye akazaa mwana, akamwita jina lake Sethi,[c] kwa sababu, kama alivyosema: "Mungu amenichagulia uzao mwingine badala ya Abeli, kwa sababu Kaini alimuua."[d] **26** Na Sethi akazaa mwana pia naye akamwita jina lake Enoshi.[e] Wakati huo watu wakaanza kuliitia jina la Yehova.[f]

5 Hiki ndicho kitabu cha historia ya Adamu. Siku ile Mungu alipomuumba Adamu alimfanya kwa mfano wa Mungu.[g] **2** Mwanamume na mwanamke aliwaumba.[h] Baada ya hapo akawabariki, akawaita jina lao Mwanadamu[i] siku ile walipoumbwa.[j]

3 Naye Adamu akaishi miaka 130. Ndipo akazaa mwana kwa mfano wake, kwa sura yake. Akamwita jina lake Sethi.[k] **4** Siku za Adamu baada ya kumzaa Sethi zikawa miaka 800. Wakati uleule akazaa wana na mabinti.[l] **5** Kwa hiyo siku zote ambazo Adamu aliishi zikajumlika kuwa miaka 930, naye akafa.[m]

SURA 4
a Kum 28:65; Met 28:17; Ho 9:17
b Ayu 34:29; Isa 59:2; Mik 3:4
c Zb 36:11
d Ro 12:19
e Mwa 4:24; Kum 32:35; Ebr 10:30
f Eze 9:6
g Zb 34:16
h Mwa 5:4
i 2Sa 18:18; Zb 49:11
j Mwa 25:27; Ebr 11:9
k Mwa 13:7; Kum 3:19
l Zb 33:2; 1Ko 14:7
m Ayu 21:12; Zb 150:4

Safu ya 2
a Kum 27:5; 2Sa 12:31; Isa 2:4
b Mwa 4:15; Law 19:18
c Mwa 5:3
d Mwa 4:8; Mt 23:35; Ebr 11:4
e Mwa 5:6; Lu 3:38
f Kut 20:7; 2Fa 19:16

SURA 5
g Mwa 1:26; 1Ko 11:7; Yak 3:9
h Mwa 1:27; Mk 10:6
i Mwa 7:21; Mhu 3:21; Mdo 17:30; 1Ko 15:39
j Mwa 1:27; Mwa 2:23; Kum 4:32; Isa 45:12; Mt 19:4
k Mwa 4:25; 1Nya 1:1
l Mwa 6:1
m Mwa 2:17; Mwa 3:19; Zb 146:4; Met 21:16; Mhu 6:6; Mhu 9:5; Eze 18:4; Ro 6:23; 1Ko 15:22

6 Naye Sethi akaishi miaka
105. Ndipo akamzaa Enoshi.[a]
7 Na baada ya kumzaa Enoshi,
Sethi akaishi miaka 807. Waka-
ti uleule akazaa wana na mabi-
nti. **8** Basi siku zote za Sethi
zikawa miaka 912, naye akafa.
9 Enoshi akaishi miaka 90.
Ndipo akamzaa Kenani.[b]
10 Na baada ya kumzaa Kena-
ni, Enoshi akaishi miaka 815.
Wakati uleule akazaa wana na
mabinti. **11** Basi siku zote za
Enoshi zikawa miaka 905, naye
akafa.
12 Naye Kenani akaishi mi-
aka 70. Ndipo akamzaa Maha-
laleli.[c] **13** Na baada ya kumzaa
Mahalaleli, Kenani akaishi mi-
aka 840. Wakati uleule akazaa
wana na mabinti. **14** Basi siku
zote za Kenani zikawa miaka
910, naye akafa.
15 Naye Mahalaleli akaishi
miaka 65. Ndipo akamzaa Yare-
di.[d] **16** Na baada ya kumzaa
Yaredi, Mahalaleli akaishi mi-
aka 830. Wakati uleule aka-
zaa wana na mabinti. **17** Basi
siku zote za Mahalaleli zikawa
miaka 895, naye akafa.
18 Na Yaredi akaishi miaka
162. Ndipo akamzaa Enoko.[e]
19 Na baada ya kumzaa Eno-
ko, Yaredi akaishi miaka 800.
Wakati uleule akazaa wana na
mabinti. **20** Basi siku zote za
Yaredi zikawa miaka 962, naye
akafa.
21 Na Enoko akaishi miaka
65. Ndipo akamzaa Methu-
sela.[f] **22** Na baada ya kumzaa
Methusela, Enoko akaende-
lea kutembea pamoja na Mu-
ngu wa kweli miaka 300. Wa-
kati uleule akazaa wana na
mabinti. **23** Basi siku zote
za Enoko zikawa miaka 365.
24 Naye Enoko akaendelea ku-
tembea[a] pamoja na Mungu wa
kweli.[b] Kisha hakuwapo tena,
kwa maana Mungu alimchu-
kua.[c]
25 Naye Methusela akaishi
miaka 187. Ndipo akamzaa La-
meki.[d] **26** Na baada ya kumzaa
Lameki, Methusela akaishi mi-
aka 782. Wakati uleule akazaa
wana na mabinti. **27** Basi siku
zote za Methusela zikawa miaka
969, naye akafa.
28 Naye Lameki akaishi mi-
aka 182. Ndipo akamzaa mwa-
na. **29** Naye akamwita jina
lake Noa,[e] akisema: "Huyu ata-
tuletea faraja katika kazi yetu
na katika maumivu ya miko-
no yetu yanayoletwa na udo-
ngo ambao Yehova amelaani."[f]
30 Na baada ya kumzaa Noa,
Lameki akaishi miaka 595. Wa-
kati uleule akazaa wana na ma-
binti. **31** Basi siku zote za La-
meki zikawa miaka 777, naye
akafa.
32 Naye Noa akafikia umri
wa miaka 500. Baada ya hapo
Noa akazaa Shemu,[g] Hamu[h] na
Yafethi.[i]

6 Sasa ikawa kwamba hesa-
bu ya wanadamu ilipoa-
nza kuongezeka usoni pa nchi
nao wakazaa mabinti,[j] **2** ndi-
po wana wa Mungu wa kwe-
li[k] wakaanza kuwaona[l] mabinti
wa wanadamu, kwamba ni we-
nye sura ya kupendeza; nao wa-
kajichukulia wake, yaani,
wote waliowachagua. **3** Baa-
da ya hapo Yehova akasema:
"Roho yangu[m] haitavumiliana
sikuzote[n] na mwanadamu kwa
kuwa yeye pia ni mwili.[o] Kwa
hiyo siku zake zitakuwa mi-
aka 120."[p]
4 Wanefili walikuwa dunia-
ni siku hizo, na pia baada ya
hapo, wakati wana wa Mungu

SURA 5
a Mwa 4:26
Lu 3:38
b 1Nya 1:2
c Lu 3:37
d 1Nya 1:2
Lu 3:37
e 1Nya 1:3
Yud 14
f 1Nya 1:3
Lu 3:37

Safu ya 2
a Kum 8:6
Amu 2:22
Zb 15:2
Met 2:7
Mik 6:8
Kol 1:10
1Th 2:12
3Yo 4
b Mwa 6:9
Kum 13:4
Yud 14
Yud 15
c Kum 34:6
Yoh 3:13
Ebr 11:5
d 1Nya 1:3
Lu 3:36
e Mwa 7:1
Eze 14:14
Mt 24:37
Ebr 11:7
1Pe 3:20
2Pe 2:5
f Mwa 3:17
g Mwa 10:21
Mwa 11:10
Lu 3:36
h Mwa 6:10
Mwa 10:6
i Mwa 10:2
Mwa 10:21

SURA 6
j Mwa 1:28
k Ayu 1:6
Ayu 38:7
2Pe 2:4
Yud 6
l Ayu 31:1
Yak 1:14
m Ro 9:22
1Pe 3:20
n Mwa 7:4
o Zb 78:39
Yoh 3:6
p Ro 9:22
1Pe 3:20
2Pe 3:9

wa kweli walipoendelea kulala
na binti za wanadamu nao wa-
kawazalia wana, hao ndio wali-
okuwa watu wenye nguvu wa
kale, wanaume wenye sifa.

5 Basi Yehova akaona kuwa
ubaya wa mwanadamu uliku-
wa mwingi duniani na kila
mwelekeo[a] wa fikira za moyo
wake ulikuwa mbaya tu wa-
kati wote.[b] **6** Yehova akaju-
ta[c] kwamba amewafanya wa-
nadamu duniani, naye akaumia
moyoni[d] mwake. **7** Kwa hiyo
Yehova akasema: "Nitawafuti-
lia mbali kutoka usoni pa nchi
wanadamu ambao nimeumba,[e]
mwanadamu na mnyama wa
kufugwa, na mnyama anayete-
mbea na kiumbe kinachoruka
cha mbinguni,[f] kwa sababu ni-
najuta kwamba nimevifanya."[g]
8 Lakini Noa akapata kibali
machoni pa Yehova.

9 Hii ndiyo historia ya Noa.
Noa alikuwa mtu mwadili-
fu.[h] Alionekana kuwa mtu asi-
ye na kosa kati ya watu wa siku
zake. Noa alitembea pamoja na
Mungu wa kweli.[i] **10** Baada
ya muda Noa akazaa wana wa-
tatu, Shemu, Hamu na Yafethi.[j]
11 Na dunia ikaharibika ma-
choni pa Mungu wa kweli,[k] du-
nia ikajaa jeuri.[l] **12** Basi Mu-
ngu akaiona dunia na, tazama!
ilikuwa imeharibika,[m] kwa sa-
babu kila mwenye mwili aliku-
wa amejiharibia njia yake duni-
ani.[n]

13 Baada ya hapo Mungu
akamwambia Noa: "Mwisho
wa wote wenye mwili umeku-
ja mbele zangu,[o] kwa maana
dunia imejaa jeuri kwa sababu
yao; na tazama mimi ninawaha-
ribu pamoja na dunia.[p] **14** Ji-
fanyie safina ya mti wenye uto-
mvu.[q] Nawe utafanya vyumba
katika safina hiyo, nawe ui-
funike kwa lami[a] ndani na nje.
15 Na hivi ndivyo utakavyoifa-
nya: urefu wa safina utakuwa
mikono[b] 300, upana wake miko-
no 50, na kimo chake kitaku-
wa mikono 30. **16** Utaifanyia
safina *tsohari* [paa; au, diri-
sha], nawe utaikamilisha kiasi
cha mkono mmoja kwenda juu,
na mwingilio wa safina utauwe-
ka katika ubavu[c] wake; utaifa-
nya ikiwa na ghorofa ya chini,
ghorofa ya pili na ghorofa ya
tatu.

17 "Tazama, mimi ninaleta
gharika[d] ya maji duniani ili ku-
haribu kutoka chini ya mbi-
ngu wote wenye mwili walio
na nguvu za uhai ndani yao.[e]
Kila kitu kilicho duniani kita-
kata pumzi.[f] **18** Nami ninafa-
nya agano langu pamoja nawe;
nawe uingie ndani ya safina,
wewe na wana wako na mke
wako na wake za wana wako
pamoja nawe.[g] **19** Na kati ya
kila kiumbe hai cha mwili
wa aina yote,[h] wawili wa kila
aina utawaleta ndani ya safi-
na ili kuwahifadhi hai pamoja
nawe.[i] Watakuwa dume na jike.
20 Kati ya viumbe vinavyo-
ruka kulingana na aina zake
na wanyama wa kufugwa ku-
lingana na aina zake,[j] kati ya
wanyama wote wanaotembea
katika nchi kulingana na aina
zake, wawili wa kila aina wata-
ingia humo pamoja nawe ili
kuwahifadhi hai.[k] **21** Wewe
nawe, jichukulie kila aina ya
chakula kinacholiwa;[l] nawe uji-
kusanyie, kiwe chakula kwa
ajili yako na kwa ajili yao."[m]

22 Naye Noa akafanya kuli-
ngana na yote ambayo Mungu
alikuwa amemwamuru. Alifa-
nya vivyo hivyo.[n]

SURA 6

a Mwa 8:21
Yak 3:15
b Mhu 7:29
Yer 17:9
Mt 15:19
c Kut 32:14
1Sa 15:11
d Zb 78:40
Zb 95:10
e Mwa 1:27
Mwa 5:1
Kum 4:32
f Mwa 7:3
g Ho 4:3
h Mwa 7:1
Eze 14:14
Ebr 11:7
i Zb 37:37
Lu 1:6
2Pe 2:5
j Mwa 5:32
k Ebr 4:13
l Zb 11:5
m Ufu 11:18
n Mt 24:38
2Pe 2:5
o Eze 7:2
Amo 8:2
1Pe 4:7
p Mwa 7:4
q Ebr 11:7

Safu ya 2

a Mwa 14:10
Kut 2:3
b Mwa 7:20
Kum 3:11
c Mwa 7:16
d Mwa 1:7
Mwa 7:6
Mt 24:39
2Pe 2:5
e Mwa 7:15
Mhu 3:19
f Mwa 7:21
Zb 104:29
g Mwa 7:13
Isa 26:20
h Mwa 8:17
1Ko 15:39
i 1Pe 3:20
j Mwa 1:25
Mwa 7:14
k Mwa 7:15
l Mwa 1:30
Isa 11:7
m Mwa 1:29
n Kut 40:16
Ebr 11:7
1Yo 5:3

7 Kisha Yehova akamwambia
Noa: "Ingia ndani ya safi-
na, wewe pamoja na nyumba
yako yote,[a] kwa maana nime-
kuona wewe kuwa mwadilifu
mbele zangu kati ya kizazi
hiki.[b] **2** Kati ya kila mnya-
ma aliye safi ujichukulie saba
saba, dume na jike lake;[c] na
kati ya kila mnyama asiye safi
wawili tu, dume na jike lake;
3 pia kati ya viumbe vinavyo-
ruka vya mbinguni saba saba,
dume na jike,[d] ili kuhifadhi
hai uzao juu ya uso wa dunia[e]
yote. **4** Kwa maana baada ya
siku 7 nitanyesha mvua[f] du-
niani siku 40 mchana na usi-
ku;[g] nami nitafutilia mbali ku-
toka uso wa nchi kila kitu kili-
choko ambacho nimekifanya."[h]
5 Basi Noa akafanya kulinga-
na na yote ambayo Yehova ali-
kuwa amemwamuru.

6 Naye Noa alikuwa na umri
wa miaka mia sita wakati gha-
rika ya maji ilipokuja dunia-
ni.[i] **7** Basi Noa akaingia nda-
ni ya safina, yeye na wanawe
na mke wake na wake za wana-
we pamoja naye, kabla ya maji
ya gharika.[j] **8** Kati ya kila
mnyama aliye safi na kati ya
kila mnyama ambaye si safi
na kati ya viumbe vinavyoruka
na kila kitu kinachotembea juu
ya nchi,[k] **9** wakaingia wawili
wawili kwa Noa ndani ya safi-
na, dume na jike, kama vile Mu-
ngu alivyokuwa amemwamuru
Noa. **10** Ikawa kwamba siku
saba baadaye maji ya gharika
yakaja juu ya dunia.

11 Katika mwaka wa mia
sita wa maisha ya Noa, mwezi
wa pili, siku ya kumi na saba
ya mwezi, katika siku hiyo che-
mchemi zote za kilindi kiku-
bwa cha maji zilitobolewa na
malango ya mbinguni yakafu-
nguliwa.[a] **12** Na hiyo mvua
kubwa juu ya dunia ikaende-
lea kwa siku 40,[b] mchana na
usiku. **13** Siku hiyohiyo Noa
akaingia ndani ya safina, yeye
na Shemu na Hamu na Yafe-
thi, wana wa Noa,[c] na mke wa
Noa na wake watatu wa wa-
nawe pamoja naye;[d] **14** wao
na kila mnyama-mwitu kuli-
ngana na aina yake,[e] na kila
mnyama wa kufugwa kulinga-
na na aina yake, na kila mnya-
ma anayetembea atembeaye
juu ya dunia kulingana na aina
yake,[f] na kila kiumbe kinacho-
ruka kulingana na aina yake,[g]
kila ndege, kila kiumbe chenye
mabawa.[h] **15** Nao wakazidi
kumwendea Noa ndani ya safi-
na, wawili wawili, kati ya kila
namna ya mwili ambamo nda-
ni yake nguvu za uhai zilikuwa
zikitenda.[i] **16** Na wale walio-
kuwa wakiingia, dume na jike
wa kila namna ya mwili, waka-
ingia, kama vile Mungu alivyo-
kuwa amemwamuru. Kisha Ye-
hova akafunga mlango nyuma
yake.[j]

17 Na hiyo gharika ikaende-
lea siku 40 juu ya dunia, na
maji yakazidi kuongezeka na
kuanza kuiinua safina nayo
ikawa inaelea juu ya dunia.
18 Maji yakazidi mno na kuen-
delea kuongezeka sana juu
ya dunia, lakini safina ilien-
delea kuelea juu ya uso wa
maji.[k] **19** Maji yakazidi mno
duniani hivi kwamba milima
yote mirefu ambayo ilikuwa
chini ya mbingu zote ikafuni-
kwa.[l] **20** Maji yakaizidi mno
milima hiyo kufikia kiasi cha
mikono kumi na mitano, kisha
ikafunikwa.[m]

SURA 7

a Met 11:21
2Pe 2:5

b Zb 91:14
Zb 101:6
Mal 3:18
Ebr 10:38
1Pe 3:12
2Pe 2:9

c Law 11:3
Kum 14:4

d Mwa 8:19

e Mwa 7:23

f Mwa 2:5
Ayu 37:6

g Mwa 7:12

h Mwa 2:19
Mwa 6:7
Mwa 6:17

i Mwa 8:13

j Lu 17:27
Ebr 11:7

k Mwa 6:20

Safu ya 2

a Mwa 1:7
Mwa 8:2

b 1Fa 19:8

c Mwa 9:18
1Nya 1:4

d Mwa 6:18
1Pe 3:20
2Pe 2:5

e Mwa 1:24

f Mwa 6:7

g Law 11:14

h Mwa 9:10

i Mwa 6:17
Zb 146:4
Mhu 3:19

j Isa 26:20

k Zb 69:15

l Ayu 12:15
2Pe 3:6

m Zb 104:6

21 Basi kila chenye mwili kilichokuwa kikitembea
juu ya dunia kikakata pumzi,[a]
kati ya viumbe vinavyoruka
na kati ya wanyama wa kufugwa na kati ya wanyama-mwitu na kati ya viumbe vyote vilivyokuwa vinazaana kwa wingi juu ya dunia, na wanadamu
wote.[b] **22** Kila kitu ambacho
ndani yake pumzi ya nguvu
za uhai ilikuwa ikitenda katika mianzi ya pua yake, yaani,
vyote ambavyo vilikuwa katika
nchi kavu, vikafa.[c] **23** Basi
akafutilia mbali kila kitu kilicho hai ambacho kilikuwa juu
ya uso wa nchi, mwanadamu na
mnyama, na mnyama anayetembea na kiumbe kinachoruka
cha mbinguni, navyo vikafutiliwa mbali duniani;[d] na Noa peke
yake na wale waliokuwa pamoja naye ndani ya safina wakaendelea kuwa hai.[e] **24** Na maji
yakaendelea kuizidi mno dunia
kwa siku 150.

8 Kisha Mungu akamkumbuka[f] Noa na kila mnyama-
mwitu na kila mnyama wa kufugwa ambaye alikuwa pamoja
naye ndani ya safina.[g] Mungu
akafanya upepo upite juu ya
dunia, nayo maji yakaanza kupungua.[h] **2** Nazo chemchemi
za kilindi cha maji[i] na malango[j]
ya mbinguni zikafungwa, na
kwa hiyo mvua kubwa kutoka
mbinguni ikazuiliwa. **3** Nayo
maji yakaanza kupungua kutoka juu ya dunia, yakapungua
hatua kwa hatua; na mwishoni
mwa siku 150 maji hayakuwapo.[k] **4** Katika mwezi wa saba,
siku ya kumi na saba ya mwezi, safina[l] ikatua kwenye milima ya Ararati.[m] **5** Na maji yakazidi kupungua hatua kwa
hatua mpaka mwezi wa kumi.

SURA 7
a Mwa 6:17
b Lu 17:27
c Mwa 6:17
Mwa 7:15
Ayu 27:3
Mhu 3:19
Isa 42:5
d Mwa 6:7
e Met 2:21
Mt 24:37
1Pe 3:20
2Pe 2:9
2Pe 3:6

SURA 8
f Mwa 19:29
Kut 2:24
1Sa 1:19
Zb 94:14
g Mwa 6:20
Ebr 11:7
h Zb 33:7
i Mwa 7:11
Met 8:28
j 2Fa 7:2
k Ayu 38:11
Yer 5:22
l Mwa 7:18
m 2Fa 19:37

Safu ya 2
a Mwa 7:20
b Mwa 6:16
c Mwa 6:20
Law 11:15
1Fa 17:4
Ayu 38:41
d Zb 55:6
e Mwa 7:19
f Ne 8:15
g Mwa 7:20
Mwa 8:3
h Yer 48:28
i Mwa 7:11
j Mwa 1:9
k Kut 14:21

Katika mwezi wa kumi, siku
ya kwanza ya mwezi, vilele vya
milima vikaonekana.[a]
6 Basi ikawa kwamba mwishoni mwa siku 40 Noa akafungua dirisha[b] la safina ambalo
alikuwa amelifanyiza. **7** Baada ya hapo akatuma kunguru,[c]
naye akaruka-ruka nje, akienda na kurudi, mpaka maji yalipokauka kutoka juu ya dunia.
8 Baadaye akatuma njiwa[d]
nje ili kuona ikiwa maji yalikuwa yamepungua kutoka katika uso wa nchi. **9** Na yule njiwa hakupata mahali popote
pa kupumzisha wayo wa mguu
wake. Basi akamrudia katika
safina kwa sababu bado maji
yalikuwako juu ya uso wa dunia yote.[e] Kwa hiyo akaunyoosha mkono wake na kumchukua. Akamwingiza ndani ya safina. **10** Naye akaendelea kungoja siku saba tena, na mara
nyingine tena akamtuma yule
njiwa nje ya safina. **11** Baadaye yule njiwa akamjia karibu
na wakati wa jioni na, tazama!
jani bichi la mzeituni[f] lilikuwa
katika mdomo wake. Basi Noa
akajua kwamba maji yalikuwa
yamepungua kutoka juu ya dunia.[g] **12** Naye akaendelea kungoja siku saba tena. Ndipo
akamtuma yule njiwa, lakini
hakurudi kwake tena kamwe.[h]
13 Basi katika mwaka wa
mia sita na moja,[i] mwezi wa
kwanza, siku ya kwanza ya
mwezi, ikawa kwamba maji
yalikuwa yamepungua kutoka
juu ya dunia; Noa akakiondoa
kifuniko cha safina akaona,
na tazama, uso wa nchi ulikuwa umekauka kabisa.[j] **14** Na
katika mwezi wa pili, siku ya 27
ya mwezi, dunia ilikuwa imekauka.[k]

15 Sasa Mungu akasema na
Noa, akamwambia: **16** "Toka
nje ya safina, wewe na mke
wako na wana wako na wake
za wana wako pamoja nawe.[a]
17 Kila kiumbe hai kilicho pa-
moja nawe chenye mwili wa
kila namna,[b] kati ya viumbe
vinavyoruka[c] na kati ya wa-
nyama[d] na kati ya wanyama
wote wanaotembea ambao hu-
tembea juu ya dunia,[e] toka nao
nje, kwa kuwa wanapaswa ku-
jaa duniani, wazaane na kuwa
wengi duniani."[f]
18 Ndipo Noa akatoka nje,
na wanawe[g] pia na mke
wake na wake za wanawe pa-
moja naye. **19** Kila kiumbe
hai, kila mnyama anayetembea
na kila kiumbe kinachoruka,
kila kitu kinachotembea juu
ya dunia, kulingana na fami-
lia zao walitoka nje ya safina.[h]
20 Noa akamjengea Yehova ma-
dhabahu[i] na kuchukua baadhi
ya wanyama wote walio safi[j] na
baadhi ya viumbe vyote vina-
vyoruka ambavyo ni safi,[k] aka-
toa matoleo ya kuteketezwa juu
ya ile madhabahu.[l] **21** Na Ye-
hova akaanza kunusa haru-
fu ya kutuliza,[m] na kwa hiyo
Yehova akasema moyoni mwa-
ke:[n] "Sitailaani nchi[o] tena ka-
mwe kwa sababu ya mwanada-
mu, kwani mwelekeo[p] wa moyo
wa mwanadamu ni mbaya tan-
gu ujana wake na kuendelea;[q]
nami sitakipiga tena kamwe
kila kitu chenye uhai kama vile
nilivyofanya.[r] **22** Siku zote
ambazo dunia inaendelea ku-
wapo, kupanda mbegu na kuvu-
na, baridi na joto, majira ya ki-
angazi na majira ya baridi kali,
mchana na usiku, havitakoma
kamwe."[s]

SURA 8

a Mwa 7:7
1Pe 3:20
2Pe 2:5
b Mwa 7:15
1Ko 15:39
c Mwa 1:20
Mwa 2:19
Mwa 6:20
d Mwa 1:25
e Mwa 1:24
Mwa 9:2
f Mwa 1:22
Zb 144:13
g Mwa 6:10
h Mwa 7:14
Zb 36:6
i Mwa 12:7
Mwa 22:9
Mwa 26:25
j Mwa 7:2
Law 20:25
Kum 14:4
k Kum 14:11
l Law 1:10
Law 1:14
Law 17:11
Kum 27:6
m Law 26:31
Eze 20:41
Efe 5:2
Ebr 13:16
n Mwa 6:6
o Mwa 3:17
Mwa 5:29
p Kum 31:21
1Nya 28:9
q Mwa 6:5
Mhu 7:20
Mt 15:19
r Mwa 6:17
Isa 54:9
s Mwa 1:14
Mhu 1:4
Yer 33:20

Safu ya 2

SURA 9

a Mwa 1:28
Mwa 8:17
b Mwa 1:26
Yak 3:7
c 1Ti 4:3
d Mwa 1:29
e Mwa 1:30
Law 17:11
Law 17:14
f Law 17:10
g Law 3:17
Law 7:26
Law 17:13
Kum 12:16
Kum 12:23
Mdo 15:20
Mdo 15:29
Mdo 21:25
h Mwa 4:10
Kut 21:12
Hes 35:31
Ufu 19:2
i Kut 20:13
Hes 35:12
Hes 35:30
Kum 19:6
2Sa 4:11
Mt 24:30
Ufu 21:8
j Mwa 1:28
Mwa 10:32
k Mwa 9:15
Isa 54:9
l Mwa 6:18
Mwa 9:18
m Mwa 8:1
Mwa 8:17

9 Naye Mungu akambariki
Noa na wanawe, akawaam-
bia: "Zaeni, muwe wengi, mja-
ze dunia.[a] **2** Kila kiumbe hai
cha dunia na kila kiumbe kina-
choruka cha mbinguni kita-
wahofu na kuwaogopa ninyi,
na pia kila kitu kinachotembea
juu ya nchi, na samaki wote
wa baharini. Vimetiwa mko-
noni mwenu.[b] **3** Kila mnya-
ma anayetembea ambaye yuko
hai anaweza kuwa chakula che-
nu.[c] Kama nilivyowapa mi-
mea ya majani, nawapeni hao
wote.[d] **4** Isipokuwa tu nya-
ma pamoja na nafsi[e] yake
—damu[f] yake—msile.[g] **5** Na,
tena, damu ya nafsi zenu nita-
itaka. Kwa mkono wa kila ki-
umbe kilicho hai nitaitaka;
na kwa mkono wa mwanada-
mu, kwa mkono wa kila mmo-
ja ambaye ni ndugu yake, ni-
taitaka nafsi ya mwanadamu.[h]
6 Yeyote anayemwaga damu
ya mwanadamu, damu yake
nayo itamwagwa na mwanada-
mu,[i] kwa maana kwa mfano wa
Mungu alimfanya mwanadamu.
7 Nanyi, zaeni na kuwa wengi,
mjaze dunia na kuwa wengi
ndani yake."[j]
8 Tena Mungu akamwa-
mbia Noa na wanawe pamo-
ja naye: **9** "Tazama, mimi
nafanya agano[k] langu pamo-
ja nanyi na pamoja na wazao
wenu baada yenu,[l] **10** na pa-
moja na kila nafsi iliyo hai
ambayo iko pamoja nanyi, kati
ya ndege, kati ya wanyama
na kati ya viumbe vyote vi-
livyo hai vya dunia ambavyo
viko pamoja nanyi, kuanzia
vyote vinavyotoka katika safi-
na mpaka kila kiumbe kilicho
hai cha dunia.[m] **11** Ndiyo, ni-
nafanya agano langu pamoja

nanyi: Mwili wote hautakatiliwa mbali tena kwa maji ya gharika, wala hakutatokea tena gharika ya kuiharibu dunia."[a]

12 Kisha Mungu akasema tena: "Hii ndiyo ishara[b] ya agano ambalo ninaweka kati yangu nanyi na kila nafsi iliyo hai ambayo iko pamoja nanyi, kwa vizazi vyote hata wakati usio na kipimo. **13** Ninawapa upinde wangu wa mvua[c] katika wingu, nao utakuwa ishara ya agano lililo kati yangu na dunia. **14** Na itakuwa kwamba ninapoleta wingu juu ya dunia, ndipo upinde wa mvua utakapoonekana katika wingu hilo. **15** Nami nitalikumbuka agano langu[d] ambalo liko kati yangu nanyi na kila nafsi iliyo hai kati ya wote wenye mwili;[e] na maji hayatakuwa gharika tena ili kuuharibu mwili wote.[f] **16** Nao upinde wa mvua utatokea katika wingu,[g] nami nitauona na kulikumbuka agano la mpaka wakati usio na kipimo[h] kati ya Mungu na kila nafsi iliyo hai kati ya mwili wote ulio duniani."[i]

17 Naye Mungu akamwambia tena Noa: "Hiyo ndiyo ishara ya agano ambalo naweka kati yangu na wote wenye mwili walio duniani."[j]

18 Wana wa Noa[k] waliotoka katika safina walikuwa Shemu na Hamu na Yafethi. Baadaye Hamu akamzaa Kanaani.[l] **19** Hao watatu walikuwa wana wa Noa, na kutokana nao watu wote wa dunia walienea kotekote.[m]

20 Sasa Noa akaanza kuwa mkulima,[n] akapanda shamba la mizabibu.[o] **21** Akanywa divai na kulewa.[p] Akajifunua katikati ya hema lake. **22** Baadaye Hamu[a] baba ya Kanaani akauona uchi wa baba yake[b] naye akaenda kuwaambia ndugu zake wawili waliokuwa nje.[c] **23** Ndipo Shemu na Yafethi wakachukua nguo ya kujitanda[d] na kuiweka kwenye mabega yao mawili. Wakatembea kinyume-nyume. Wakaufunika uchi wa baba yao, nyuso zao zikiwa zimegeuzwa, nao hawakuuona uchi wa baba yao.[e]

24 Mwishowe Noa akaamka kutoka katika divai yake akapata kujua jambo ambalo mwana wake mdogo alikuwa amemfanyia. **25** Basi akasema:

"Alaaniwe Kanaani.[f]
Na awe mtumwa wa hali ya chini kabisa kwa ndugu zake."[g]

26 Naye akasema tena:

"Abarikiwe Yehova,[h]
Mungu wa Shemu,
Kanaani na awe mtumwa wake.[i]
27 Mungu na ampe Yafethi nafasi ya kutosha,
Akae katika mahema ya Shemu.[j]
Kanaani na awe mtumwa wake pia."

28 Na Noa akaendelea kuishi miaka 350 baada ya gharika.[k] **29** Basi siku zote za Noa zikawa miaka 950, naye akafa.[l]

10 Na hii ndiyo historia ya wana wa Noa,[m] yaani, Shemu, Hamu na Yafethi.

Sasa wakaanza kuzaa wana baada ya gharika.[n] **2** Wana wa Yafethi walikuwa Gomeri[o] na Magogu[p] na Madai[q] na Yavani[r] na Tubali[s] na Mesheki[t] na Tirasi.[u]

3 Na wana wa Gomeri walikuwa Ashkenazi[v] na Rifathi[w] na Togarma.[x]

SURA 9

a Mwa 8:21
b Kut 3:12
c Eze 1:28 Ufu 4:3
d Law 26:42 Isa 54:9
e 1Ko 15:39
f Mwa 8:21
g Ayu 38:36
h Zb 105:8 Zb 111:5
i Kum 7:9 Ebr 6:18
j Mwa 9:13
k Mwa 5:32 Mwa 7:7 Mwa 10:1
l Mwa 10:6
m 1Nya 1:4 1Pe 3:20
n Mwa 2:15 2Ti 2:6
o Kum 20:6
p Mwa 19:35 Met 23:35

Safu ya 2

a 1Nya 1:8
b Law 18:7 Eze 22:10
c Met 12:13 Met 17:9 Efe 5:3
d Mwa 37:34 Kut 22:27
e Kut 20:12 Law 19:32 Isa 58:7
f Law 18:3 Kum 7:1 Kum 27:16 Ro 1:27
g Yos 17:13
h Kut 18:10 Kum 8:10 1Fa 1:48 1Nya 29:20 Lu 1:68
i Yos 9:23 Amu 1:28 1Fa 9:21
j 1Nya 1:5
k Mwa 7:6
l Ebr 11:7

SURA 10

m 1Nya 1:4 Lu 3:36
n Mwa 9:19
o Eze 38:6 Ga 1:2
p Eze 38:2
q 2Fa 17:6 Isa 13:17
r Zek 9:13
s Isa 66:19 Eze 27:13
t Zb 120:5 Eze 32:26
u 1Nya 1:5
v Yer 51:27
w 1Nya 1:6
x Eze 27:14 Eze 38:6

4 Na wana wa Yavani walikuwa Elisha[a] na Tarshishi,[b] Kitimu[c] na Dodanimu.[d]
5 Kutokana na hawa, watu wa visiwa vya mataifa wakaenea kotekote katika nchi zao, kila mmoja kulingana na lugha yake, kulingana na familia zao, kulingana na mataifa yao.

6 Na wana wa Hamu walikuwa Kushi[e] na Misraimu[f] na Putu[g] na Kanaani.[h]

7 Na wana wa Kushi walikuwa Seba[i] na Havila na Sabta na Raama[j] na Sabteka.

Na wana wa Raama walikuwa Sheba na Dedani.[k]

8 Na Kushi akamzaa Nimrodi.[l] Akawa wa kwanza kuwa mwenye nguvu duniani. **9** Akajionyesha kuwa mwindaji mwenye nguvu kwa kumpinga Yehova. Hiyo ndiyo sababu kuna msemo: "Kama tu Nimrodi, mwindaji mwenye nguvu kwa kumpinga Yehova."[m] **10** Nao mwanzo wa ufalme wake ukawa Babeli[n] na Ereki[o] na Akadi na Kalne, katika nchi ya Shinari.[p] **11** Akatoka katika nchi ile akaingia Ashuru[q] na kuanza kujenga Ninawi[r] na Rehoboth-Iri na Kala. **12** na Reseni kati ya Ninawi na Kala: hili ndilo lile jiji kubwa.

13 Naye Misraimu[s] akamzaa Ludimu[t] na Anamimu na Lehabimu na Naftuhimu[u] **14** na Pathrusimu[v] na Kasluhimu[w] (ambao Wafilisti[x] walitokana nao) na Kaftorimu.[y]

15 Naye Kanaani akamzaa Sidoni,[z] mzaliwa wake wa kwanza, na Hethi[a] **16** na Myebusi[b] na Mwamori[c] na Mgirgashi **17** na Mhivi[d] na Mwarkia na Msini **18** na Mwarvadi[e] na Msemari na Mhamathi;[a] baadaye familia za Mkanaani zikatawanyika. **19** Basi mpaka wa Mkanaani ukawa kutoka Sidoni mpaka Gerari,[b] karibu na Gaza,[c] mpaka Sodoma na Gomora[d] na Adma[e] na Seboiimu,[f] karibu na Lasha. **20** Hao ndio waliokuwa wana wa Hamu kulingana na familia zao, kulingana na lugha zao, katika nchi zao, kulingana na mataifa yao.

21 Naye Shemu, babu ya wana wote wa Eberi,[g] ndugu ya Yafethi mkubwa kuliko wote, pia alizaa watoto. **22** Wana wa Shemu walikuwa Elamu[h] na Asihuru[i] na Arpakshadi[j] na Ludi na Aramu.

23 Na wana wa Aramu walikuwa Usi na Huli na Getheri na Mashi.[k]

24 Naye Arpakshadi akamzaa Shela,[l] na Shela akamzaa Eberi.

25 Naye Eberi alizaa wana wawili. Jina la mmoja lilikuwa Pelegi,[m] kwa sababu katika siku zake dunia ilikuwa imegawanyika;[n] na jina la ndugu yake lilikuwa Yoktani.[o]

26 Naye Yoktani akazaa Almodadi na Shelefu na Hazarmavethi na Yera[p] **27** na Hadoramu na Uzali na Dikla[q] **28** na Obali na Abimaeli na Sheba[r] **29** na Ofiri[s] na Havila[t] na Yobabu;[u] hao wote ndio waliokuwa wana wa Yoktani.

30 Na mahali pao pa kukaa pakaenea kutoka Mesha mpaka Sefari, eneo lenye milima la Mashariki.

31 Hawa ndio waliokuwa wana wa Shemu kulingana na

SURA 10

a Eze 27:7
b 1Fa 10:22
Yon 1:3
c Isa 23:1
d 1Nya 1:7
e 1Nya 1:8
f Mwa 50:11
g Yer 46:9
Nah 3:9
h Hes 34:2
i Zb 72:10
j Eze 27:22
k 1Nya 1:9
l 1Nya 1:10
m Zb 35:4
n Mwa 11:9
o Ezr 4:9
p Da 1:2
q Mik 5:6
r Yon 3:3
Mt 12:41
s 1Nya 1:8
t Yer 46:9
u 1Nya 1:11
v Eze 29:14
w 1Nya 1:12
x Yos 13:3
Yer 47:4
y Kum 2:23
z Yos 13:6
Mk 7:24
a Mwa 25:10
Mwa 27:46
b Amu 1:21
c Mwa 15:16
Kum 3:8
d Yos 11:3
e Eze 27:11

Safu ya 2

a 1Fa 8:65
Zek 9:2
b Mwa 20:1
c Yos 15:47
Mdo 8:26
d Mwa 13:10
Mwa 19:24
2Pe 2:6
Yud 7
e Kum 29:23
f Mwa 14:8
g Mwa 11:17
h Ezr 4:9
Mdo 2:9
i Eze 27:23
j Mwa 11:10
k 1Nya 1:17
l Mwa 11:12
Lu 3:35
m Mwa 11:16
n Mwa 11:9
o 1Nya 1:19
p 1Nya 1:20
q 1Nya 1:21
r 1Nya 1:22
s 1Fa 9:28
1Fa 10:11
1Nya 29:4
t Mwa 2:11
Mwa 25:18
u 1Nya 1:23

familia zao, kulingana na lugha
zao, katika nchi zao, kulingana
na mataifa yao.[a]

32 Hizi ndizo zilizokuwa fa-
milia za wana wa Noa kulinga-
na na ukoo wa familia zao, ku-
lingana na mataifa yao, na ku-
tokana nao mataifa yakaenea
kotekote duniani baada ya gha-
rika.[b]

11 Sasa dunia yote iliende-
lea kuwa na lugha moja
na maneno ya namna moja.
2 Mwishowe ikawa kwamba
walipokuwa wakisafiri kue-
lekea mashariki, waligundua
nchi tambarare ya bondeni
katika nchi ya Shinari,[c] nao
wakakaa huko. **3** Nao waka-
anza kuambiana: "Haya! Na tu-
tengeneze matofali tuyacho-
me." Basi matofali yakawa
mawe yao, lakini lami ikawa
saruji yao.[d] **4** Ndipo wakase-
ma: "Haya! Na tujijengee jiji na
pia mnara na kilele chake kiwe
mbinguni,[e] na tujifanyie jina
maarufu,[f] tusije tukatawanyi-
ka juu ya uso wote wa dunia."[g]
5 Yehova akashuka aone jiji
na mnara ambao wanadamu
walikuwa wamejenga.[h] **6** Ha-
lafu Yehova akasema: "Tazama!
Wao ni kikundi kimoja
cha watu na wote wana lu-
gha moja,[i] na hivi ndivyo wa-
navyoanza kufanya. Basi sasa
hakuna chochote wanacho-
wazia akilini mwao kufanya
kitakachowashinda kufikia.[j]
7 Haya! Na tushuke,[k] tuvu-
ruge[l] lugha yao huko ili wa-
siweze kusikilizana lugha."[m]
8 Basi Yehova akawatawanya
juu ya uso wote wa dunia ku-
toka huko,[n] nao pole kwa
pole wakaacha kulijenga lile
jiji.[o] **9** Hiyo ndiyo sababu lili-
itwa jina lake Babeli,[a] kwa sa-
babu huko ndiko Yehova aliku-
wa amevuruga lugha ya dunia
yote, na kutoka huko Yehova
alikuwa amewatawanya[b] juu ya
uso wote wa dunia.

10 Hii ndiyo historia ya
Shemu.[c]

Shemu alikuwa na umri wa
miaka 100 wakati alipomzaa
Arpakshadi[d] miaka miwili
baada ya gharika. **11** Na baa-
da ya kumzaa Arpakshadi,
Shemu akaishi miaka 500. Wa-
kati uleule akazaa wana na ma-
binti.[e]

12 Naye Arpakshadi akaishi
miaka 35. Ndipo akamzaa She-
la.[f] **13** Na baada ya kumzaa
Shela, Arpakshadi akaishi mi-
aka 403. Wakati uleule akazaa
wana na mabinti.

14 Naye Shela akaishi mia-
ka 30. Ndipo akamzaa Eberi.[g]
15 Na baada ya kumzaa Eberi,
Shela akaishi miaka 403. Waka-
ti uleule akazaa wana na mabi-
nti.

16 Naye Eberi akaishi mia-
ka 34. Ndipo akamzaa Pelegi.[h]
17 Na baada ya kumzaa Pelegi,
Eberi akaishi miaka 430. Waka-
ti uleule akazaa wana na mabi-
nti.

18 Naye Pelegi akaishi mi-
aka 30. Ndipo akamzaa Reu.[i]
19 Na baada ya kumzaa Reu,
Pelegi akaishi miaka 209. Wa-
kati uleule akazaa wana na ma-
binti.

20 Naye Reu akaishi mia-
ka 32. Ndipo akamzaa Serugi.[j]
21 Na baada ya kumzaa Seru-
gi, Reu akaishi miaka 207. Wa-
kati uleule akazaa wana na ma-
binti.

22 Naye Serugi akaishi mia-
ka 30. Ndipo akamzaa Nahori.[k]

SURA 10
a Mwa 10:5
b Mwa 9:7
Mwa 9:19
Mdo 17:26

SURA 11
c Mwa 10:10
Da 1:2
d Kut 1:14
Kut 2:3
e Amo 9:2
f Zb 49:11
Da 4:30
Yoh 5:44
g Mwa 9:1
Lu 1:51
h Mwa 18:21
Zb 11:4
Ebr 4:13
i Mwa 11:1
j Mhu 7:29
1Ko 1:19
k Mwa 1:26
Met 8:30
l Ayu 5:12
Zb 33:10
Zb 55:9
m Mwa 10:5
n Kum 32:8
Lu 1:51
o Ayu 12:14
Zb 127:1

Safu ya 2
a Yer 50:1
1Pe 5:13
b Zb 68:30
Lu 1:51
c Mwa 6:10
1Nya 1:4
Lu 3:36
d Mwa 10:22
1Nya 1:17
e Mwa 10:21
f Mwa 10:24
1Nya 1:18
Lu 3:35
g Mwa 10:21
1Nya 1:18
h Mwa 10:25
1Nya 1:19
i 1Nya 1:25
Lu 3:35
j Lu 3:35
k 1Nya 1:26

23 Na baada ya kumzaa Nahori, Serugi akaishi miaka 200. Wakati uleule akazaa wana na mabinti.

24 Naye Nahori akaishi miaka 29. Ndipo akamzaa Tera.[a] **25** Na baada ya kumzaa Tera, Nahori akaishi miaka 119. Wakati uleule akazaa wana na mabinti.

26 Naye Tera akaishi miaka 70, kisha akamzaa Abramu,[b] Nahori[c] na Harani.

27 Na hii ndiyo historia ya Tera.

Tera akamzaa Abramu, Nahori na Harani; naye Harani akamzaa Loti.[d] **28** Baadaye Harani akafa akiwa angali na baba yake Tera katika nchi ya kuzaliwa kwake, katika Uru[e] la Wakaldayo.[f] **29** Nao Abramu na Nahori wakajichukulia wake. Jina la mke wa Abramu lilikuwa Sarai,[g] na jina la mke wa Nahori lilikuwa Milka[h] binti ya Harani, baba ya Milka na baba ya Iska. **30** Lakini Sarai aliendelea kuwa tasa;[i] hakuwa na mtoto.

31 Baada ya hapo Tera akamchukua mwana wake Abramu, na mjukuu wake Loti,[j] mwana wa Harani, na binti-mkwe wake Sarai,[k] mke wa mwana wake Abramu, nao wakaondoka Uru la Wakaldayo pamoja naye ili kwenda katika nchi ya Kanaani.[l] Baadaye wakaja Harani[m] na kukaa huko. **32** Na siku za Tera zikawa miaka 205. Ndipo Tera akafa huko Harani.

12 Naye Yehova akamwambia Abramu: "Nenda zako kutoka katika nchi yako na kutoka kwa watu wa jamaa yako na kutoka kwa nyumba ya baba yako mpaka katika nchi ambayo nitakuonyesha;[a] **2** nami nitafanya taifa kubwa kutokana nawe, nitakubariki na kulifanya jina lako kuwa kuu; nawe uwe baraka.[b] **3** Nami nitawabariki wale wanaokubariki, na yule anayekulaani nitamlaani,[c] na familia zote za nchi zitajibariki kupitia kwako."[d]

4 Ndipo Abramu akaenda kama vile Yehova alivyokuwa amemwambia, na Loti akaenda pamoja naye. Na Abramu alikuwa na umri wa miaka 75 alipoondoka Harani.[e] **5** Basi Abramu akamchukua Sarai mke wake[f] na Loti mwana wa ndugu yake[g] na mali zote ambazo walikuwa wamekusanya[h] na nafsi ambazo walikuwa wamejipatia katika Harani, nao wakaenda nchi ya Kanaani.[i] Mwishowe wakafika katika nchi ya Kanaani. **6** Na Abramu akapita katikati ya nchi mpaka eneo la Shekemu,[j] karibu na miti mikubwa ya More;[k] wakati huo Mkanaani alikuwa katika nchi hiyo. **7** Ndipo Yehova akamtokea Abramu na kusema: "Nitaupa uzao wako[l] nchi hii."[m] Baada ya hayo akajenga madhabahu huko kwa ajili ya Yehova, aliyekuwa amemtokea. **8** Baadaye akaondoka huko kwenda katika eneo lenye milima upande wa mashariki wa Betheli.[n] Akapiga hema lake, Betheli likiwa upande wa magharibi, na Ai[o] upande wa mashariki. Ndipo akamjengea Yehova madhabahu huko[p] naye akaanza kuliitia jina la Yehova.[q] **9** Baadaye Abramu akavunja kambi, wakati huo akienda

SURA 11
a Mwa 11:32; Lu 3:34
b Mwa 12:7; Mwa 15:6; Mwa 17:5; Mwa 18:19; Yoh 8:39; Ro 4:11; Ga 3:16; Ebr 11:17; Yak 2:23
c Yos 24:2
d Mwa 12:4; Mwa 19:1; 2Pe 2:7
e Mwa 15:7; Ne 9:7
f 2Fa 24:2; Mdo 7:4
g Mwa 12:11; Mwa 17:15; Mwa 20:12; 1Pe 3:6
h Mwa 22:20; Mwa 24:15
i Mwa 16:2; Mwa 18:11; Ro 4:19; Ebr 11:11
j Mwa 11:27
k Mwa 12:5; Mwa 16:1
l Mwa 9:26; Mwa 10:19; Mwa 12:7; Hes 34:2; Mdo 13:19
m Mwa 12:4; Mwa 27:43; Mdo 7:2

Safu ya 2

SURA 12
a Yos 24:3; Mdo 7:4
b Mwa 13:16; Mwa 15:5; Mwa 17:5; Mwa 22:17; Ebr 6:14
c Mwa 27:29; Kut 23:22; Hes 24:9
d Zek 8:23; Lu 1:73; Mdo 3:25; Ga 3:8
e Ebr 11:8
f Mwa 11:29
g Mwa 11:31
h Mwa 13:6; Mhu 5:19
i Mwa 26:3; Mdo 7:16
j Mdo 7:16
k Mwa 35:4; Kum 11:30
l Mwa 3:15; Mwa 21:12; Mwa 28:14; Ro 9:7; Ga 3:16
m Mwa 13:15; Mwa 15:7; Mwa 17:8; Kum 34:4
n Mwa 28:19; Mwa 31:13
o Mwa 13:3; Yos 7:2
p Mwa 8:20; Mwa 35:3
q Mwa 26:25; Met 18:10; Ro 10:13

kutoka kambi mpaka kambi
kuelekea Negebu.[a]
10 Sasa njaa ikatokea kati-
ka nchi, naye Abramu akate-
remka kuelekea Misri akakae
huko akiwa mgeni,[b] kwa saba-
bu njaa ilikuwa kali katika
nchi.[c] **11** Ikawa mara alipo-
karibia kuingia Misri, akamwa-
mbia Sarai mke wake: "Tafa-
dhali, tazama! najua vema
kuwa wewe ni mwanamke
mwenye sura nzuri.[d] **12** Basi
itakuwa kwamba Wamisri wa-
takapokuona watasema, 'Huyu
ni mke wake.' Nao wataniua, la-
kini wewe watakuhifadhi hai.
13 Tafadhali sema wewe ni
dada yangu,[e] ndipo iwe vema
kwangu kwa sababu yako, na
nafsi yangu itaishi kwa ajili
yako."[f]
14 Basi ikawa kwamba,
mara Abramu alipoingia Mi-
sri, Wamisri wakapata ku-
mwona mwanamke huyo, kwa-
mba alikuwa mrembo sana.
15 Na wakuu wa Farao pia
wakapata kumwona nao wa-
kaanza kumsifu mbele ya
Farao, basi mwanamke huyo
akapelekwa nyumbani kwa Fa-
rao. **16** Naye akamtendea
Abramu vema kwa sababu
yake, naye akawa na kondoo
na ng'ombe na punda na wa-
tumishi wa kiume na wajaka-
zi na punda-jike na ngamia.[g]
17 Ndipo Yehova akamgusa
Farao na nyumba yake kwa
mapigo makubwa[h] kwa saba-
bu ya Sarai, mke wa Abramu.[i]
18 Basi Farao akamwita Abra-
mu na kusema: "Ni nini hili
umenitendea? Kwa nini huku-
niambia kwamba yeye ni mke
wako?[j] **19** Kwa nini ulisema,
'Yeye ni dada yangu,'[k] basi ni-
kawa karibu kumchukua awe
mke wangu? Basi mke wako
ndiye huyu. Mchukue, uende!"
20 Ndipo Farao akawatolea
watu amri kumhusu, nao waka-
msindikiza yeye na mke wake
na vyote alivyokuwa navyo.[a]

13 Baada ya hayo Abramu
akaondoka Misri, yeye
na mke wake na vyote ali-
vyokuwa navyo, na Loti pa-
moja naye, kwenda Negebu.[b]
2 Naye Abramu alikuwa na
utajiri mwingi wa mifugo na
fedha na dhahabu.[c] **3** Naye
akaenda kambi kwa kambi ku-
toka Negebu mpaka Betheli,
kwenda mahali ambapo hema
lake lilikuwa mara ya kwanza
kati ya Betheli na Ai,[d] **4** pe-
nye madhabahu ambayo aliku-
wa ameifanya hapo mwanzoni;[e]
naye Abramu akaliitia jina la
Yehova hapo.[f]
5 Sasa Loti pia, aliyekuwa
akienda pamoja na Abramu,
alikuwa na kondoo na ng'ombe
na mahema. **6** Basi nchi ha-
ikuwaruhusu wakae wote pa-
moja, kwa sababu mali zao zili-
kuwa zimekuwa nyingi nao
hawakuweza kukaa pamoja.[g]
7 Na ugomvi ukatokea kati ya
wachungaji wa mifugo ya Abra-
mu na wachungaji wa mifugo
ya Loti; na wakati huo Mkana-
ani na Mperizi walikuwa waki-
kaa katika nchi hiyo.[h] **8** Ndi-
po Abramu akamwambia Loti:[i]
"Tafadhali, usiruhusu ugomvi
wowote uendelee kuwa kati ya-
ngu na wewe na kati ya wa-
chungaji wangu na wachungaji
wako, kwa kuwa sisi ni ndugu.[j]
9 Je, nchi yote haiko mbele
yako? Tafadhali, jitenge nami.
Ukienda kushoto, mimi nita-
kwenda kuume; lakini ukie-
nda kuume, mimi nitakwenda

SURA 12
a Mwa 20:1
Mwa 24:62
b Mwa 47:4
Kum 23:7
Zb 105:13
Mdo 7:6
c Mwa 26:1
d Mwa 26:7
e Mwa 12:19
f Mwa 20:12
g Mwa 20:14
Mwa 24:35
h 1Sa 5:11
i Mwa 11:29
Mwa 17:15
Mwa 23:19
j Ro 7:3
k Mwa 20:2
Mwa 20:12

Safu ya 2
a Zb 105:14

SURA 13
b Mwa 12:9
Mwa 20:1
c Mwa 24:35
Kum 8:18
d Mwa 12:8
Yos 7:2
e Mwa 12:7
f Mwa 21:33
Isa 12:4
Ro 10:13
g Mwa 36:7
h Mwa 10:19
Mwa 15:18
i Mwa 11:27
j Zb 133:1
Met 15:18
Ro 12:10

kushoto.”[a] **10** Basi Loti akainua macho yake na kuona Wilaya yote ya Yordani,[b] kwamba yote ilikuwa eneo lililokuwa na maji mengi kabla Yehova hajaharibu Sodoma na Gomora, kama bustani ya Yehova,[c] kama nchi ya Misri mpaka Soari.[d] **11** Ndipo Loti akajichagulia Wilaya yote ya Yordani. Loti akahamisha kambi yake kuelekea mashariki. Basi wakatengana. **12** Abramu alikaa katika nchi ya Kanaani, lakini Loti akakaa kati ya majiji ya Wilaya hiyo.[e] Mwishowe akapiga hema karibu na Sodoma. **13** Basi watu wa Sodoma walikuwa wabaya nao walikuwa wakimtendea Yehova dhambi nzito.[f]

14 Yehova akamwambia Abramu baada ya Loti kujitenga naye: “Tafadhali, inua macho yako utazame kutoka mahali ulipo, upande wa kaskazini na wa kusini na wa mashariki na wa magharibi,[g] **15** kwa kuwa nchi yote ambayo unaitazama, nitakupa wewe na uzao wako hata wakati usio na kipimo.[h] **16** Nami nitaufanya uzao wako uwe kama chembe za mavumbi ya dunia, ili, ikiwa mwanadamu angeweza kuzihesabu chembe za mavumbi ya dunia, basi uzao wako ungeweza kuhesabiwa.[i] **17** Ondoka, zunguka katika nchi kwa marefu na mapana yake, kwa kuwa hiyo nitakupa wewe.”[j] **18** Basi Abramu akaendelea kuishi katika mahema. Baadaye akaja na kukaa kati ya miti mikubwa ya Mamre,[k] ambayo iko katika Hebroni;[l] na huko akamjengea Yehova madhabahu.[m]

SURA 13
a Met 17:14; Ro 12:18; Ebr 12:14
b Mwa 19:28
c Mwa 2:9; Isa 51:3; Eze 36:35
d Mwa 19:22
e Mwa 19:29
f Mwa 18:20; Mwa 19:5; Ro 1:27; 2Pe 2:6; Yud 7
g Kum 34:1
h Mwa 12:7; Mwa 15:18; Mwa 24:7; Kut 33:1
i Mwa 12:2; Mwa 15:5; Kut 1:7; Kum 26:5; Ebr 11:12
j Kum 34:4; Yos 12:7
k Mwa 18:1; Mwa 23:19; Mwa 25:9
l Mwa 23:2
m Mwa 12:7

Safu ya 2

SURA 14
a Mwa 10:10
b Mwa 14:17
c Mwa 10:22
d Mwa 14:9
e Mwa 10:19; Mwa 13:12; 2Pe 2:6
f Mwa 13:10; Mwa 18:20; Yud 7
g Ho 11:8
h Kum 29:23
i Kum 34:3
j Amu 20:11
k Mwa 14:10
l Kum 3:17
m Kum 1:4
n Kum 2:10
o Kum 2:12
p Mwa 36:8
q Mwa 21:21
r Hes 20:1
s Mwa 36:12; 1Sa 15:2
t Mwa 10:16
u 2Nya 20:2
v Mwa 14:3
w Mwa 14:1

14 Sasa ikawa siku za Amrafeli mfalme wa Shinari,[a] Arioko mfalme wa Elasari, Kedorlaoma[b] mfalme wa Elamu,[c] na Tidali mfalme wa Goiimu,[d] **2** kwamba hao wakafanya vita na Bera mfalme wa Sodoma,[e] na Birsha mfalme wa Gomora,[f] Shinabu mfalme wa Adma,[g] na Shemeberi mfalme wa Seboiimu,[h] na mfalme wa Bela (yaani, Soari).[i] **3** Hao wote wakaenda pamoja kwa kushirikiana[j] mpaka katika Nchi Tambarare ya Chini ya Sidimu,[k] yaani, Bahari ya Chumvi.[l]

4 Walikuwa wamemtumikia Kedorlaoma miaka kumi na miwili, lakini mwaka wa kumi na tatu wakaasi. **5** Na mwaka wa kumi na nne Kedorlaoma akaja, na pia wafalme waliokuwa pamoja naye, nao wakashinda Warefaimu katika Ashteroth-karnaimu,[m] na Wazuzi katika Hamu, na Waemi[n] katika Shave-kiriathaimu, **6** na Wahori[o] katika mlima wao wa Seiri,[p] mpaka El-parani,[q] ulioko nyikani. **7** Ndipo wakageuka na kuja En-mishpati, yaani, Kadeshi,[r] wakashinda shamba lote la Waamaleki[s] na pia Waamori[t] waliokuwa wakikaa katika Hasason-tamari.[u]

8 Ndipo mfalme wa Sodoma akapiga mwendo, na pia mfalme wa Gomora na mfalme wa Adma na mfalme wa Seboiimu na mfalme wa Bela (yaani, Soari), nao wakajipanga kivita wapigane nao katika Nchi Tambarare ya Chini ya Sidimu,[v] **9** wapigane na Kedorlaoma mfalme wa Elamu na Tidali mfalme wa Goiimu na Amrafeli mfalme wa Shinari na Arioko mfalme wa Elasari;[w]

wafalme wanne wapigane na watano. **10** Basi Nchi Tambarare ya Chini ya Sidimu[a] ilikuwa imejaa mashimo ya lami;[b] nao wafalme wa Sodoma na Gomora[c] wakakimbia na kuanguka ndani yake, na wale waliobaki wakakimbilia eneo lenye milima.[d] **11** Ndipo washindi wakachukua mali zote za Sodoma na Gomora na chakula chao chote, wakaenda zao.[e] **12** Pia wakamchukua Loti mwana wa ndugu ya Abramu na mali zake, wakaenda zao. Wakati huo alikuwa akikaa Sodoma.[f]

13 Baada ya hayo mtu aliyekuwa ameponyoka akaja na kumwambia Abramu Mwebrania.[g] Wakati huo alikuwa akikaa kati ya miti mikubwa ya Mamre yule Mwamori,[h] ndugu ya Eshkoli na ndugu ya Aneri;[i] nao walikuwa washirika wa Abramu. **14** Basi Abramu akasikia kwamba ndugu yake amechukuliwa mateka.[j] Kwa hiyo akakusanya watu wake waliozoezwa,[k] watumwa mia tatu kumi na wanane waliozaliwa nyumbani mwake,[l] akawafuatilia mpaka Dani.[m] **15** Na wakati wa usiku akagawa vikosi vyake,[n] yeye na watumwa wake, kupigana nao, basi akawashinda na kuendelea kuwafuata mpaka Hoba, upande wa kaskazini wa Damasko. **16** Naye akarudisha mali zote,[o] naye akamrudisha pia Loti ndugu yake na mali zake zote na pia wanawake na watu.[p]

17 Ndipo mfalme wa Sodoma akatoka kwenda kumpokea baada ya kurudi kutoka kumshinda Kedorlaoma na wafalme waliokuwa pamoja naye, katika Nchi Tambarare ya Chini ya Shave, yaani, Nchi Tambarare ya Chini ya mfalme.[a] **18** Na Melkizedeki[b] mfalme wa Salemu[c] akaleta mkate na divai,[d] naye alikuwa kuhani wa Mungu Aliye Juu Zaidi.[e] **19** Ndipo akambariki na kusema:

> "Abarikiwe Abramu wa Mungu Aliye Juu Zaidi,[f]
> Yeye aliyezitokeza mbingu na dunia;[g]
> **20** Na abarikiwe Mungu Aliye Juu Zaidi,[h]
> Ambaye amewatia wakandamizaji wako mkononi mwako!"[i]

Kisha Abramu akampa sehemu ya kumi ya kila kitu.[j]

21 Baada ya hayo mfalme wa Sodoma akamwambia Abramu: "Nipe nafsi hizo,[k] lakini ujichukulie mali." **22** Ndipo Abramu akamwambia mfalme wa Sodoma: "Nainua mkono wangu katika kiapo[l] kwa Yehova Mungu Aliye Juu Zaidi, Mtokezaji wa mbingu na dunia, **23** kwamba, wala uzi wala kamba ya kiatu, sitachukua kitu kutoka kwa chochote kilicho chako,[m] usije ukasema, 'Ni mimi niliyemtajirisha Abramu.' **24** Sitaki chochote![n] Isipokuwa tu kile ambacho vijana wamekula tayari, na fungu la watu walioenda nami, Aneri, Eshkoli na Mamre[o]—na wachukue fungu lao."[p]

15 Baada ya mambo hayo neno la Yehova likamjia Abramu katika maono,[q] na kusema: "Usiogope,[r] Abramu. Mimi ni ngao kwako.[s] Thawabu yako itakuwa kubwa sana."[t] **2** Ndipo Abramu akasema: "Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-

SURA 14
a Mwa 14:3
b Mwa 11:3
Kut 2:3
c Kum 29:23
d Mwa 19:30
e Mwa 14:16
f Mwa 19:1
2Pe 2:7
g Mwa 40:15
Kut 3:18
h Mwa 10:16
Mwa 13:18
i Mwa 14:24
Hes 32:9
j Mwa 11:27
k 1Fa 20:27
l Mwa 17:12
m Amu 18:29
n Mwa 32:7
Amu 7:16
o 1Sa 30:19
p Kut 15:13

Safu ya 2
a 2Sa 18:18
b Zb 110:4
Ebr 6:20
Ebr 7:3
Ebr 7:10
c Ebr 7:1
d Amu 19:19
e Zb 83:18
Ebr 5:10
f Ga 3:14
g Zb 115:15
Ufu 10:6
h 1Nya 29:10
i Kum 28:7
j Mwa 28:22
Ebr 7:4
k Mwa 46:15
Yer 39:18
l Kum 32:40
m Est 9:15
n Mdo 20:33
o Mwa 14:13
p Met 3:27
1Ti 5:18

SURA 15
q Kut 6:3
Hes 12:6
r Zb 27:1
Isa 41:10
Ro 8:31
Ebr 13:6
s Kum 33:29
Met 30:5
t Mwa 17:6
Ebr 11:6

hova, utanipa nini, kwa sababu
mimi naenda zangu bila mto-
to na yule atakayeirithi nyu-
mba yangu ni Eliezeri,[a] mtu
wa Damasko?" **3** Kisha Abra-
mu akasema tena: "Tazama! Hu-
kunipa uzao[b] wowote, na, taza-
ma! mwana[c] wa nyumba ya-
ngu anakuwa mrithi wangu."
4 Lakini, tazama! neno la Yeho-
va likamjia kwa maneno haya:
"Mtu huyu hatakuwa mrithi
wako, lakini yule atakayeto-
ka katika viuno vyako mwenye-
we ndiye atakayekuwa mrithi
wako."[d]

5 Ndipo akamtoa nje na
kusema: "Tafadhali, tazama
juu mbinguni uzihesabu nyo-
ta, ikiwa unaweza kuzihesa-
bu."[e] Naye akaendelea kumwa-
mbia: "Ndivyo utakavyoku-
wa uzao wako."[f] **6** Naye aka-
wa na imani katika Yehova;[g]
naye akamhesabia kuwa ni
uadilifu.[h] **7** Ndipo akaonge-
za kumwambia: "Mimi ni Yeho-
va, niliyekutoa katika Uru la
Wakaldayo ili nikupe nchi hii
uirithi."[i] **8** Akajibu akasema:
"Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova, nitajuaje kwamba nitai-
rithi?"[j] **9** Naye akamwambia:
"Nichukulie ndama wa miaka
mitatu na mbuzi-jike wa mia-
ka mitatu na kondoo-dume wa
miaka mitatu na njiwa-tetere
na njiwa mchanga."[k] **10** Basi
akawachukua wote hao na ku-
wakata vipande viwili. Akawe-
ka kila kipande chao ili kili-
ngane na kile kingine, lakini
wale ndege hakuwakata vipa-
nde.[l] **11** Na ndege wawindaji
wakaanza kushuka juu ya mizo-
ga hiyo,[m] lakini Abramu akawa
akiwafukuza.

12 Baada ya muda fulani jua
likawa karibu kutua, na usi-

SURA 15
a Mwa 24:2
b Mwa 12:7
Mdo 7:5
c Kut 2:10
d Mwa 21:12
e Yer 33:22
f Mwa 22:17
Kum 1:10
Ebr 11:12
g Ro 4:18
Ebr 11:8
Yak 2:23
h Ro 4:13
Ro 4:22
Ga 3:6
i Mwa 11:31
Ne 9:7
Zb 105:11
j Amu 6:17
Lu 1:18
k Law 1:14
l Law 1:17
m Law 11:13

Safu ya 2
a 1Sa 26:12
b Kum 10:19
Ebr 11:13
c Mwa 21:9
Kut 1:14
Kut 3:7
Mdo 7:6
d Kut 7:4
Hes 33:4
e Kut 3:22
Zb 105:37
f Mwa 25:8
g Yos 14:1
Mdo 7:7
h 1Fa 21:26
2Fa 21:11
1Th 2:16
i 1Nya 21:26
Yer 34:18
j Mwa 17:19
Mwa 22:17
Ga 3:17
k Kut 3:8
l 1Fa 4:21
m 1Sa 15:6
n Yos 1:4
o Kut 3:17
p Yos 17:15
q Kum 7:1

SURA 16
r Mwa 15:3
s Mwa 12:16
Ga 4:25
t Mwa 20:17
u Mwa 30:3

ngizi mzito ukamshika Abra-
mu,[a] na, tazama! giza kubwa la
kuogopesha likaanza kumwa-
ngukia. **13** Naye akaanza ku-
mwambia Abramu: "Ujue haki-
ka kwamba uzao wako utaku-
wa mkaaji mgeni katika nchi
isiyokuwa yao,[b] nao watawatu-
mikia watu wale, nao wata-
watesa kwa miaka mia nne.[c]
14 Lakini taifa watakalolitu-
mikia mimi ninalihukumu,[d]
na baada ya hapo wataondo-
ka na mali nyingi.[e] **15** Laki-
ni wewe, utaenda kwa mababu
zako kwa amani; utazikwa ka-
tika uzee mwema.[f] **16** Lakini
katika kizazi cha nne watarudi
hapa,[g] kwa sababu kosa la Wa-
amori halijawa kamili bado."[h]

17 Basi jua lilikuwa likitua
na giza kubwa likaja na, taza-
ma! kulikuwa na tanuru lina-
lotoa moshi na mwenge wenye
moto uliokuwa ukipita katika-
ti ya vipande hivyo.[i] **18** Siku
hiyo Yehova akafanya agano
na Abramu,[j] akisema: "Nitau-
patia uzao wako nchi hii,[k] ku-
toka mto wa Misri mpaka
ule mto mkubwa, mto Efra-
ti:[l] **19** Wakeni[m] na Wakenizi
na Wakadmoni **20** na Wahi-
ti[n] na Waperizi[o] na Warefaimu[p]
21 na Waamori na Wakanaani
na Wagirgashi na Wayebusi."[q]

16 Sasa Sarai, mke wa
Abramu, hakuwa ame-
mzalia watoto wowote;[r] laki-
ni alikuwa na mjakazi Mmi-
sri na jina lake lilikuwa Ha-
gari.[s] **2** Ndipo Sarai akamwa-
mbia Abramu: "Tafadhali sasa!
Yehova amenifunga nisizae wa-
totoo.[t] Tafadhali, lala na mjaka-
zi wangu. Labda ninaweza ku-
pata watoto kutokana naye."[u]
Basi Abramu akaisikiliza sauti

ya Sarai.[a] **3** Ndipo Sarai, mke
wa Abramu, akamchukua Ha-
gari, mjakazi wake Mmisri,
mwishoni mwa miaka kumi
ya kukaa kwa Abramu kati-
ka nchi ya Kanaani, naye aka-
mpa mume wake Abramu
kama mke wake.[b] **4** Basi aka-
lala na Hagari, naye akapata
mimba. Wakati alipojua kwa-
mba ana mimba, ndipo bimku-
bwa wake akawa mtu wa ku-
dharaulika machoni pake.[c]

5 Basi Sarai akamwambia
Abramu: "Jeuri niliyotendewa
na iwe juu yako. Mimi nilimtia
mjakazi wangu kifuani pako,
naye alipojua kwamba ana mi-
mba, akaanza kunidharau ma-
choni pake. Yehova na ahu-
kumu kati yangu na wewe."[d]
6 Ndipo Abramu akamwambia
Sarai:[e] "Tazama! Mjakazi wako
yuko chini ya mamlaka yako.
Mtendee yaliyo mema macho-
ni pako."[f] Basi Sarai akaanza
kumfedhehesha hivi kwamba
akakimbia kutoka kwake.[g]

7 Baadaye malaika wa Ye-
hova[h] akamkuta kwenye che-
mchemi ya maji nyikani, kwe-
nye chemchemi iliyo njiani
kuelekea Shuri.[i] **8** Naye aka-
anza kusema: "Hagari, mja-
kazi wa Sarai, umetoka wapi
nawe unaenda wapi?" Naye
akajibu: "Mimi ninakimbia ku-
toka kwa Sarai bimkubwa wa-
ngu." **9** Na malaika wa Yeho-
va akaendelea kumwambia:
"Rudi kwa bimkubwa wako
ujinyenyekeze chini ya mko-
no wake."[j] **10** Ndipo malai-
ka wa Yehova akamwambia:
"Nitauzidisha sana uzao wako,[k]
hivi kwamba hautahesabiwa
kwa sababu ya wingi wake."[l]
11 Tena, malaika wa Yehova
akamwambia: "Tazama una mi-
mba, nawe utazaa mwana,
nawe utamwita jina lake Ishma-
eli;[a] kwa kuwa Yehova ameyasi-
kia mateso yako.[b] **12** Na yeye
atakuwa kama punda-milia.
Mkono wake utamwinukia kila
mtu, na mkono wa kila mtu uta-
mwinukia yeye;[c] naye atakaa
mbele ya uso wa ndugu zake
wote."[d]

13 Ndipo akaanza kuliita
jina la Yehova, aliyekuwa aki-
sema naye: "Wewe ni Mungu
mwenye kuona,"[e] kwa kuwa
alisema: "Je, kweli hapa nime-
mtazama yeye anayeniona?"
14 Hiyo ndiyo sababu kisima
hicho kiliitwa Beer-lahai-roi.[f]
Tazama, kiko kati ya Kadeshi
na Beredi. **15** Baadaye Haga-
ri akamzalia Abramu mwana
naye Abramu akamwita huyo
mwana wake ambaye Hagari
alimzalia, jina lake Ishmaeli.[g]
16 Naye Abramu alikuwa na
umri wa miaka 86 Hagari alipo-
mzalia Ishmaeli.

17 Abramu alipokuwa na
umri wa miaka 99, Yeho-
va akamtokea Abramu na ku-
mwambia:[h] "Mimi ni Mungu
Mweza-Yote.[i] Tembea mbele
zangu nawe ujionyeshe kuwa
huna kosa.[j] **2** Nami nitaweka
agano langu kati yangu mimi
na wewe,[k] ili nipate kukuzidi-
sha wewe sana sana."[l]

3 Ndipo Abramu akaangu-
ka kifudifudi,[m] na Mungu aka-
endelea kusema naye, na ku-
mwambia: **4** "Kwa habari ya-
ngu, tazama! agano langu lipo
pamoja na wewe,[n] nawe hakika
utakuwa baba ya umati wa
mataifa.[o] **5** Na jina lako hali-
takuwa Abramu tena, jina lako
litakuwa Abrahamu, kwa saba-
bu nitakufanya kuwa baba ya

SURA 16
a Mwa 21:12
Efe 5:21
b Mwa 30:9
c 1Sa 1:6
d Kut 5:21
1Sa 24:12
Zb 43:1
e Met 15:1
Met 15:18
f Met 29:19
g Met 15:12
Mhu 10:4
1Pe 2:20
h Mwa 22:11
i Mwa 25:18
Kut 15:22
j Mhu 10:4
Efe 6:5
Tit 2:9
k Mwa 17:20
l Mwa 25:13
1Nya 1:29
Efe 6:8

Safu ya 2
a Mwa 17:18
b Zb 22:24
c Mwa 37:28
d Mwa 21:20
e 2Nya 16:9
Met 5:21
Met 15:3
Ebr 4:13
f Mwa 24:62
g Mwa 21:9
Ga 4:24

SURA 17
h Mwa 12:7
i Ufu 16:7
j Zb 15:2
Zb 18:23
k Zb 105:8
Ga 3:17
l Mwa 22:17
Kum 1:10
Ebr 11:12
m Amu 13:20
Mt 17:6
n Zb 105:9
o Mwa 13:16
Ro 4:17

umati wa mataifa. **6** Nami nitakufanya uwe mwenye kuzaa
sana sana na kukufanya uwe
mataifa, na wafalme watatoka
ndani yako.[a]
7 "Nami nitatimiza aga-
no langu kati yangu mimi na
wewe[b] na uzao wako baada
yako kulingana na vizazi vyao
kuwa agano la mpaka waka-
ti usio na kipimo,[c] ili kujio-
nyesha mwenyewe kuwa Mu-
ngu kwako na kwa uzao wako
baada yako.[d] **8** Nami nitaku-
pa wewe na uzao wako baada
yako ile nchi ya makao yako ya
kigeni,[e] naam, nchi yote ya Ka-
naani, ili kuimiliki hata waka-
ti usio na kipimo; nami nitaji-
onyesha mwenyewe kuwa Mu-
ngu kwao."[f]
9 Na tena Mungu akamwa-
mbia Abrahamu: "Kwa habari
yako, unapaswa kushika aga-
no langu, wewe na uzao wako
baada yako kulingana na vi-
zazi vyao.[g] **10** Hili ndilo aga-
no langu ambalo ninyi mta-
shika, kati yangu na ninyi,
hata uzao wako baada yako.[h]
Kila mwanamume wa kwenu
lazima atahiriwe.[i] **11** Nanyi
mnapaswa kutahiriwa nyama
ya magovi yenu, nayo iwe isha-
ra ya agano kati yangu mimi na
ninyi.[j] **12** Na kila mwanamu-
me wa kwenu wa umri wa siku
nane lazima atahiriwe,[k] kuli-
ngana na vizazi vyenu, yeyo-
te aliyezaliwa ndani ya nyumba
na yeyote aliyenunuliwa kwa
pesa kutoka kwa mgeni yeyo-
te ambaye si wa uzao wako.
13 Kila mwanamume aliyezali-
wa ndani ya nyumba yako na
kila mwanamume aliyenunuli-
wa kwa pesa zako asikose ku-
tahiriwa;[l] na agano langu ka-
tika miili yenu ninyi wanaume
lazima litumike likiwa agano
mpaka wakati usio na kipimo.[a]
14 Na mwanamume ambaye
hajatahiriwa, ambaye hatata-
hiri nyama ya govi lake, nafsi
hiyo lazima ikatiliwe mbali ku-
toka kwa watu wake.[b] Yeye
amevunja agano langu."
15 Naye Mungu akaendelea
kumwambia Abrahamu: "Kwa
habari ya Sarai mke wako, usi-
mwite jina lake Sarai, kwa
sababu Sara ndilo jina lake.[c]
16 Nami nitambariki yeye na
pia nitakupa mwana kupi-
tia yeye;[d] nami nitambariki
Sara naye atakuwa mataifa;[e]
wafalme wa vikundi vya watu
watatoka kwake."[f] **17** Ndipo
Abrahamu akaanguka kifudi-
fudi, akaanza kucheka na ku-
sema moyoni mwake:[g] "Je, mtu
wa umri wa miaka 100 atazaa
mtoto, na je, Sara, ndiyo, je,
mwanamke wa umri wa miaka
90 atazaa?"[h]
18 Kisha Abrahamu aka-
mwambia Mungu wa kweli:
"Laiti Ishmaeli angeishi mbele
zako!"[i] **19** Basi Mungu aka-
sema: "Sara mke wako kwa
kweli atakuzalia mwana, nawe
utamwita jina lake Isaka.[j]
Nami nitafanya agano langu
pamoja naye kuwa agano la
mpaka wakati usio na kipimo
kwa uzao wake baada yake.[k]
20 Lakini kuhusu Ishmaeli ni-
mekusikia. Tazama! nitambari-
ki, nimfanye aongezeke na ku-
mzidisha sana sana.[l] Hakika
atatokeza wakuu kumi na wa-
wili, nami nitamfanya kuwa
taifa kubwa.[m] **21** Hata hivyo,
agano langu nitalifanya pamo-
ja na Isaka,[n] ambaye Sara ata-
kuzalia wakati huu uliowekwa
mwaka ujao."[o]

SURA 17
a 2Fa 1:18
b Mik 7:20
Lu 1:72
c Amu 2:1
Zb 105:10
d Kut 19:5
Mk 12:26
e Kut 6:4
Ebr 11:9
f Kum 14:2
Zb 105:11
g Kut 19:5
Kum 11:13
h Mwa 21:4
Lu 2:21
i Mwa 34:15
Yos 5:2
Ro 2:29
j Mdo 7:8
Ro 4:11
k Mwa 21:4
Lu 2:21
Flp 3:5
l Kut 12:44
Mdo 16:3

Safu ya 2
a Amu 2:1
Zb 111:5
b Kut 4:24
Hes 15:31
Yoh 7:23
c Mwa 11:29
d Mwa 18:10
Ro 9:9
e Mwa 35:11
f 2Nya 28:26
g Mwa 18:12
Mwa 21:6
Lu 2:19
h Ro 4:19
Ebr 11:11
i Mwa 16:11
j Mt 1:2
Ro 9:7
Ga 4:28
k Mwa 26:24
Zb 105:9
Lu 1:33
Ga 4:28
l Mwa 16:10
Mwa 21:13
Mwa 25:13
m Mwa 21:18
1Nya 1:29
n Mwa 26:3
Kut 2:24
Ebr 11:9
o Mwa 18:14
Mwa 21:1

22 Kwa hayo Mungu aka-
maliza kusema naye, akaenda
zake juu kutoka kwa Abra-
hamu.[a] **23** Ndipo Abrahamu
akamchukua Ishmaeli mwana
wake na wanaume wote wali-
ozaliwa nyumbani mwake na
kila mtu aliyenunuliwa kwa
pesa zake, kila mtu wa kiu-
me kati ya wanaume wa nyu-
mba ya Abrahamu, naye akaa-
nza kutahiri nyama ya magovi
yao siku hiyo hiyo, kama Mu-
ngu alivyokuwa amemwa-
mbia.[b] **24** Na Abrahamu ali-
kuwa na umri wa miaka
99 alipotahiriwa nyama ya govi
lake.[c] **25** Na Ishmaeli mwana
wake alikuwa na umri wa mi-
aka kumi na mitatu alipota-
hiriwa nyama ya govi lake.[d]
26 Siku hiyo hiyo Abrahamu
alitahiriwa, na pia Ishmaeli
mwana wake.[e] **27** Na wanau-
me wote wa nyumba yake, ye-
yote aliyezaliwa nyumbani na
yeyote aliyenunuliwa kwa pesa
kutoka kwa mgeni, alitahiriwa
pamoja naye.[f]

18 Baadaye Yehova aka-
mtokea[g] kati ya miti mi-
kubwa ya Mamre,[h] alipoku-
wa ameketi kwenye mwingi-
lio wa hema karibu na wakati
wa joto la mchana.[i] **2** Alipoi-
nua macho yake,[j] kisha aka-
tazama, kumbe pale, wamesi-
mama wanaume watatu umbali
fulani kutoka kwake. Alipowa-
ona akaanza kukimbia awa-
pokee kutoka mwingilio wa
hema naye akainama kifudi-
fudi.[k] **3** Kisha akasema: "Ye-
hova, ikiwa, sasa, nimepata
kibali machoni pako, tafadha-
li usimpite mtumishi wako.[l]
4 Tafadhali, acha maji kidogo
yachukuliwe, nanyi mwoshwe
miguu yenu.[m] Kisha mketi chi-
ni ya mti.[a] **5** Nanyi acheni ni-
chukue kipande cha mkate, ni-
burudishe mioyo yenu.[b] Baada-
ye, ninyi mnaweza kuendelea
mbele, kwa maana hiyo ndiyo
sababu mmepitia njia hii kwa
mtumishi wenu." Basi wakase-
ma: "Vema. Unaweza kufanya
kama ulivyosema."

6 Kwa hiyo Abrahamu aka-
fanya haraka kwenda katika
hema alimokuwa Sara, akase-
ma: "Fanya haraka! Chukua vi-
pimo vitatu vya sea vya unga
laini, ukande donge na kuoka
keki za mviringo."[c] **7** Kisha
Abrahamu akakimbia kwenye
mifugo akachukua ng'ombe-
dume mchanga, mzuri na mwo-
roro akampa mtumishi, naye
akafanya haraka kumtayari-
sha.[d] **8** Ndipo akachukua si-
agi na maziwa na yule ng'o-
mbe mchanga ambaye alikuwa
amemtayarisha, akaweka mbe-
le yao.[e] Kisha yeye akaendelea
kusimama kando yao chini ya
mti walipokuwa wakila.[f]

9 Sasa wakamwambia:
"Yuko wapi Sara mke wako?"[g]
Ndipo akasema: "Hapa hema-
ni!"[h] **10** Kwa hiyo akaende-
lea kusema: "Hakika mimi ni-
tarudi kwako mwaka ujao wa-
kati huu, na, tazama! Sara mke
wako atapata mwana."[i] Basi
Sara alikuwa akisikiliza kwe-
nye mwingilio wa hema, nao
ulikuwa nyuma ya mwanamu-
me huyo. **11** Naye Abrahamu
na Sara walikuwa wazee, wa-
mesonga katika miaka.[j] Sara
alikuwa ameacha kuwa na he-
dhi.[k] **12** Kwa hiyo Sara akaa-
nza kucheka ndani yake mwe-
nyewe,[l] akisema: "Baada ya
mimi kuzeeka, kweli mimi ni-
tapata raha, tena bwana wa-
ngu akiwa mzee vilevile?"[m]

SURA 17
a Kum 5:4
b Mwa 17:13
Yos 5:2
Ro 2:29
c Mdo 7:8
Ro 4:11
d Mwa 16:16
e Zb 119:60
f Kut 12:44

SURA 18
g Mwa 16:7
Amu 13:21
Mdo 7:2
h Mwa 13:18
Mwa 14:13
i Mwa 31:40
Mt 20:12
j Mwa 19:1
Mwa 22:4
k Mwa 23:7
Ru 2:10
l Mdo 16:15
m Mwa 24:32
1Sa 25:41
Yoh 13:5

Safu ya 2
a Yoh 6:10
b Zb 104:15
c Mwa 19:3
Kut 12:39
d Lu 15:23
e Kum 32:14
2Sa 17:29
f Lu 12:37
Ro 12:13
Ebr 13:2
g Mwa 17:15
h Mwa 24:67
Mwa 31:33
i Mwa 21:2
Mt 3:9
Ro 9:9
j Mwa 17:17
k Law 15:19
Ro 4:19
l Mwa 17:17
m Lu 11:27
Ebr 11:11
1Pe 3:6

13 Kisha Yehova akamwambia
Abrahamu: "Kwa nini Sara
amecheka, akisema, 'Je, kwa
hakika na kwa kweli mimi
nitazaa ingawa nimezeeka?'[a]
14 Je, jambo lolote ni kubwa
mno isivyo kawaida kwa Yeho-
va?[b] Kwa wakati uliowekwa ni-
tarudi kwako, mwaka ujao wa-
kati huu, na Sara atapata mwa-
na." **15** Lakini Sara akaanza
kukana hilo, akisema: "Mimi si-
kucheka!" Kwa maana aliogo-
pa. Ndipo yeye akasema: "Si-
vyo! ulicheka."[c]

16 Baadaye hao wanaume
wakasimama kutoka hapo wa-
katazama chini kuelekea So-
doma,[d] naye Abrahamu aliku-
wa akitembea pamoja nao ili
awasindikize.[e] **17** Naye Yeho-
vah akasema: "Je, nimfiche
Abrahamu jambo ninalofanya?[f]
18 Tazama, kwa hakika Abra-
hamu atakuwa taifa kubwa
na lenye nguvu, na mataifa
yote ya dunia yatajibariki ku-
pitia kwake.[g] **19** Kwa maa-
na nimefahamiana naye kusu-
di awaamuru wanawe na nyu-
mba yake baada yake, ndipo
washike njia ya Yehova ili kute-
nda uadilifu na haki;[h] ili Yeho-
va apate kumtimizia Abraha-
mu lile alilosema juu yake."[i]

20 Ndipo Yehova akasema:
"Kilio cha malalamiko juu ya
Sodoma na Gomora[j] ni kiku-
bwa, na dhambi yao ni nzito
sana.[k] **21** Mimi nimeazimia
kabisa kushuka ili nipate kuo-
na kama wanatenda kabisa ku-
lingana na kile kilio kilicho juu
yake ambacho kimenifikia, na
ikiwa sivyo, nitajua."[l]

22 Basi wale wanaume wa-
kageuka kutoka hapo, waka-
enda Sodoma; lakini Yehova[m]
alikuwa bado amesimama mbe-
le ya Abrahamu.[a] **23** Kisha
Abrahamu akakaribia na ku-
anza kusema: "Je, kweli uta-
fagilia mbali mwadilifu pamoja
na mwovu?[b] **24** Tuseme kuna
watu waadilifu 50 katika jiji
hilo. Je, wewe, utawafagilia
mbali, usisamehe mahali hapo
kwa ajili ya wale waadilifu
50 ambao wamo ndani yake?[c]
25 Ni jambo lisilowaziwa kwa-
ko kwamba unatenda namna
hii kuua mtu mwadilifu pamo-
ja na mwovu hivi kwamba mtu
mwadilifu apatwe na jambo li-
lelile kama ilivyo kwa mwovu![d]
Ni jambo lisilowaziwa kwako.[e]
Je, Mwamuzi wa dunia yote ha-
tafanya lililo sawa?"[f] **26** Ki-
sha Yehova akasema: "Mimi ni-
kipata katika Sodoma watu 50
waadilifu katika jiji hilo nitapa-
samehe mahali hapo pote kwa
ajili yao."[g] **27** Lakini Abraha-
mu akaendelea kujibu na kusu-
ma: "Tafadhali, tazama nimeji-
amulia kusema na Yehova, hali
mimi ni mavumbi na majivu.[h]
28 Tuseme wale 50 walio wa-
adilifu wapungue 5. Je, wewe
utaliharibu jiji zima kwa ku-
pungua hao 5?" Akajibu akase-
ma: "Mimi sitaliharibu nikipata
humo 45."[i]

29 Lakini tena akasema zai-
di naye, na kumwambia: "Tuse-
me 40 wapatikane humo." Naye
akamjibu: "Sitafanya hivyo
kwa ajili ya wale 40." **30** La-
kini yeye akaendelea kusema:
"Tafadhali, Yehova na asiwake
hasira,[j] bali acha niendelee ku-
sema:[k] Tuseme 30 wapatikane
humo." Naye akamjibu: "Mimi
sitafanya hivyo nikipata 30
humo." **31** Lakini yeye akae-
ndelea kusema: "Tafadhali, ta-
zama nimejiamulia mwenyewe
kusema na Yehova:[l] Tuseme 20

SURA 18

a Isa 40:29
b Mt 19:26
Lu 1:37
c Zb 44:21
Ebr 4:13
d Mwa 13:12
e 2Sa 19:31
Mdo 20:38
Ro 15:24
f Zb 25:14
Amo 3:7
g Mwa 12:3
Zek 8:23
Ga 3:14
h 2Sa 22:25
Zb 15:2
Met 2:9
Met 21:3
i Kum 4:9
j Met 21:13
2Pe 2:8
k Mwa 9:25
Mwa 13:13
Isa 3:9
Yud 7
l Mwa 11:5
Kut 3:7
Yos 22:22
Zb 14:2
m Mwa 31:11
Mwa 32:30
Amu 6:11

Safu ya 2

a Zb 106:23
b Mwa 20:4
Hes 16:22
Ayu 34:19
Yer 15:1
Mt 13:49
Ro 3:5
c Yer 5:1
d Zb 37:10
Met 29:16
Mal 3:18
e Kum 32:4
f Ayu 34:12
Zb 50:6
Zb 94:2
Isa 33:22
Zek 7:9
g Yer 5:1
Eze 22:30
h Mwa 3:19
Ayu 30:19
Zb 113:7
1Ko 15:47
i Hes 14:18
Zb 78:38
Isa 65:8
j Kut 34:6
Ezr 5:12
Zb 86:15
Ebr 12:29
k Ebr 4:16
l Ayu 40:4
Mt 7:7
Lu 11:8

wapatikane humo.” Naye akamjibu: “Mimi sitaliharibu kwa ajili ya wale 20.”[a] **32** Mwishowe yeye akasema: “Tafadhali, Yehova na asiwake hasira,[b] bali acha niseme mara hii moja tu:[c] Tuseme kumi wapatikane humo.” Naye akamjibu: “Mimi sitaliharibu kwa ajili ya hao kumi.”[d] **33** Kisha Yehova[e] akaenda zake alipokuwa amemaliza kusema na Abrahamu, naye Abrahamu akarudi kwake.

19 Basi wale malaika wawili wakafika Sodoma wakati wa jioni, na Loti alikuwa ameketi katika lango la Sodoma.[f] Loti alipowaona, akasimama awapokee, akainama kifudifudi.[g] **2** Naye akaanza kusema: “Tafadhali, sasa, bwana zangu, pitieni hapa, tafadhali, mwingie ndani ya nyumba ya mtumishi wenu, mkae usiku kucha, mwoshwe miguu yenu.[h] Kisha mwamke mapema, msafiri na kwenda zenu.”[i] Nao wakajibu wakasema: “Hapana, bali katika uwanja wa watu wote ndipo tutakapokaa usiku kucha.”[j] **3** Lakini akawasisitizia sana,[k] basi wakageuka na kuingia kwake, wakaingia ndani ya nyumba yake. Kisha akawafanyia karamu,[l] akaoka keki zisizo na chachu,[m] nao wakala.

4 Kabla hawajalala, wanaume wa jiji, wanaume wa Sodoma, wakaizingira nyumba,[n] kuanzia mvulana mpaka mzee, watu wote wakiwa kikundi kimoja.[o] **5** Nao wakaendelea kumwita Loti na kumwambia: “Wako wapi wale wanaume ambao waliingia kwako usiku wa leo? Walete nje kwetu ili tulale nao.”[p]

SURA 18
a Zb 9:12 Mdo 27:24
b Amu 6:39 Ebr 3:15
c Kut 4:10 Zb 86:6
d Isa 1:9 Eze 14:16
e Mwa 18:22

SURA 19
f Ru 4:1 Est 2:19
g Mwa 18:2 1Sa 24:8
h Mwa 18:4 Ayu 31:32 Yoh 13:12
i Amu 19:9 1Sa 29:10
j Amu 19:15
k Amu 19:20 Lu 24:29 Mdo 16:15
l Mwa 18:8 2Fa 6:23
m Amu 6:19 1Sa 28:24
n Amu 19:22
o Met 4:16 Efe 4:19
p Law 18:22 Law 20:13 Ro 1:27 1Ko 6:9 Yud 7

Safu ya 2
a Ro 1:24 2Pe 2:12 Yud 10
b Mwa 24:16
c Amu 19:24
d Ro 1:26 2Pe 2:9
e Kum 10:19 Amu 19:23 Isa 58:7
f Kut 22:21
g Mdo 7:27 1Pe 4:4
h Zb 118:13
i Met 14:16
j 2Fa 6:18 Mdo 13:11
k Yer 8:10
l Mhu 10:15 Mt 15:14
m Hes 16:26 1Sa 15:6 Yer 51:6
n Mwa 13:13 Mwa 18:20 Isa 3:9

6 Mwishowe, Loti akawaendea nje kwenye mwingilio, lakini akaufunga mlango nyuma yake. **7** Kisha akasema: “Tafadhali, ndugu zangu, msitende vibaya.[a] **8** Tafadhali, hapa nina binti wawili ambao hawajapata kamwe kulala na mwanamume.[b] Tafadhali, acheni niwatoe nje kwenu. Kisha mwatendee kama ilivyo vema machoni penu.[c] Ila tu wanaume hawa msiwatendee jambo,[d] kwa kuwa ndiyo sababu wamekuja chini ya kivuli cha paa yangu.”[e] **9** Nao wakajibu wakasema: “Toka hapa!” Nao wakaongeza hivi: “Mtu huyu aliye peke yake alikuja hapa kukaa akiwa mgeni[f] na sasa anajifanya kuwa mwamuzi.[g] Sasa sisi tutakutendea wewe vibaya zaidi kuliko wao.” Nao wakaja wakisongamana kwa nguvu juu ya huyo mwanamume,[h] juu ya Loti, na walikuwa wakikaribia kuuvunja mlango.[i] **10** Basi wale wanaume wakanyoosha mikono yao na kumwingiza Loti walimokuwa, ndani ya nyumba, nao wakaufunga mlango. **11** Lakini wakawapiga kwa upofu wanaume waliokuwa kwenye mwingilio wa nyumba,[j] kuanzia aliye mdogo zaidi mpaka aliye mkubwa zaidi,[k] hata wakawa wanajichosha wakijaribu kuutafuta mwingilio.[l]

12 Kisha hao wanaume wakamwambia Loti: “Je, una mtu yeyote mwingine hapa? Mwana-mkwe na wana wako na binti zako na wote walio wako jijini, watoe nje ya mahali hapa![m] **13** Kwa maana sisi tutapaharibu mahali hapa, kwa sababu kilio juu yao kimekuwa kikubwa mbele za Yehova,[n]

hivi kwamba Yehova alitutuma tuliharibu jiji.”[a] **14** Kwa hiyo Loti akatoka nje akaanza kusema na wana-wakwe zake ambao wangechukua binti zake, naye akaendelea kusema: “Ondokeni! Tokeni mahali hapa, kwa sababu Yehova ataliharibu jiji!”[b] Lakini machoni pa wana-wakwe zake alionekana kama mtu aliyekuwa anafanya mzaha.[c]

15 Hata hivyo, kulipopambazuka, malaika wakamhimiza Loti, wakisema: “Simama! Mchukue mke wako na binti zako wawili walio hapa,[d] usije ukafagiliwa mbali katika makosa ya jiji hili!”[e] **16** Alipoendelea kukawia,[f] ndipo kwa huruma za Yehova kwake,[g] wale wanaume wakaushika mkono wake na mkono wa mke wake na mikono ya binti zake wawili. Wakamtoa nje na kumweka nje ya jiji.[h] **17** Ikawa kwamba, mara tu walipokuwa wamewatoa nje ya jiji, akaanza kusema: “Kimbia kwa ajili ya nafsi yako![i] Usitazame nyuma[j] wala usisimame katika Wilaya yote![k] Kimbilia eneo lenye milima usije ukafagiliwa mbali!”[l]

18 Kisha Loti akawaambia: “Sivyo, tafadhali, Yehova! **19** Tafadhali, sasa, mtumishi wako amepata kibali machoni pako[m] hivi kwamba unatukuza fadhili zako zenye upendo,[n] fadhili ambazo umenionyesha ili kuhifadhi hai[o] nafsi yangu, lakini mimi—mimi siwezi kukimbilia eneo lenye milima kwa sababu naogopa nisije nikafikiwa na msiba nife.[p] **20** Tafadhali, sasa, jiji hili liko karibu kuweza kukimbiliwa nalo ni dogo.[q] Tafadhali, acha nikimbilie huko—je, hilo si dogo?—na nafsi yangu itaendelea kuishi.”[a] **21** Kwa hiyo yeye akamwambia: “Haya, nakujali kwa kadiri hii pia[b] kwa vile sitaliangamiza jiji ambalo umesema.[c] **22** Fanya haraka! Kimbilia huko, kwa sababu mimi siwezi kufanya jambo lolote mpaka wewe utakapofika huko!”[d] Ndiyo sababu aliliita jiji hilo Soari.[e]

23 Jua lilikuwa limetokeza juu ya nchi hiyo wakati Loti alipofika Soari.[f] **24** Ndipo Yehova akanyesha kiberiti na moto kutoka kwa Yehova, kutoka mbinguni, juu ya Sodoma na juu ya Gomora.[g] **25** Kwa hiyo akaendelea kuyaangamiza majiji hayo, hata Wilaya yote na wakaaji wote wa hayo majiji na mimea ya udongo.[h] **26** Naye mke wake akaanza kutazama nyuma, akiwa nyuma yake, naye akawa nguzo ya chumvi.[i]

27 Sasa Abrahamu akaondoka asubuhi na mapema kwenda mahali alipokuwa amesimama mbele za Yehova.[j] **28** Kisha akatazama chini kuelekea Sodoma na Gomora na kuelekea nchi yote ya Wilaya hiyo, akaona ajabu. Kumbe, tazama moshi mzito ulikuwa ukipanda kutoka nchi hiyo kama moshi mzito wa tanuru![k] **29** Ikawa kwamba Mungu alipoharibu majiji ya Wilaya hiyo, Mungu alimkumbuka Abrahamu, kwa kuwa alichukua hatua za kumwondoa Loti kutoka katikati ya hayo maangamizi alipokuwa akiyaangamiza majiji ambayo kati yake Loti alikuwa amekaa.[l]

30 Baadaye Loti akatoka Soari, akaanza kukaa pamoja

SURA 19

a 1Nya 21:15; Zb 11:6; Mt 13:41
b Hes 16:45; Ufu 18:4
c 2Nya 36:16; Lu 17:28
d Lu 17:31
e Hes 16:26
f Ro 12:11
g Kut 33:19; Yoe 2:18
h Yos 6:23; 2Pe 2:9
i 1Sa 19:11
j Lu 9:62; Flp 3:13
k Mwa 13:10; Yer 45:5; Yer 51:50
l Mt 24:16; Ebr 2:3
m Mwa 18:3; Amu 6:17
n Kut 15:13; Mik 7:18
o Zb 41:2; Zb 143:11
p Zb 6:4; Mt 8:25
q 2Fa 3:18

Safu ya 2

a Zb 68:20; Zb 119:175
b Zb 34:15
c Mwa 19:30
d Hab 2:3; 2Pe 3:9; Ufu 7:3
e Mwa 14:2
f Mwa 19:27
g Kum 29:23; Zb 11:6; Isa 1:9; Amo 4:11; Lu 17:29; 2Pe 2:6
h Mwa 13:10; Zb 107:34; Yer 49:18; Sef 2:9
i Lu 17:32; Ebr 10:38
j Mwa 18:22
k Yud 7
l 2Pe 2:7

na binti zake wawili katika
eneo lenye milima,[a] kwa sa-
babu aliogopa kukaa Soari.[b]
Kwa hiyo yeye na binti zake
wawili wakaanza kukaa pa-
ngoni. **31** Naye yule mzali-
wa wa kwanza akamwambia
yule mwanamke mdogo: "Baba
yetu ni mzee na hakuna mwa-
namume yeyote katika nchi
hii wa kulala nasi kulinga-
na na njia ya dunia nzima.[c]
32 Njoo, tumpe baba yetu divai
anywe[d] nasi tulale naye. Ndi-
po tuhifadhi uzao kutoka kwa
baba yetu."[e]

33 Basi wakaendelea kumpa
baba yao divai anywe usiku
huo;[f] kisha mzaliwa wa kwa-
nza akaingia ndani akalala na
baba yake, lakini yeye haku-
jua wakati binti yake alipolala
na wakati alipoamka. **34** Ika-
wa kwamba kesho yake mzali-
wa wa kwanza akamwambia
yule mdogo: "Haya, mimi ni-
lilala na baba yangu usiku wa
jana. Tumpe divai anywe usi-
ku wa leo pia. Kisha wewe ui-
ngie ndani ulale naye, ili tu-
hifadhi uzao kutoka kwa baba
yetu." **35** Kwa hiyo wakampa
tena na tena baba yao divai
anywe usiku huo pia; Kisha
yule mdogo akaondoka, akalala
naye, lakini yeye hakujua waka-
ti binti yake alipolala na wakati
alipoamka. **36** Na binti wote
wawili wa Loti wakapata mi-
mba kutoka kwa baba yao.[g]
37 Baada ya muda yule mzali-
wa wa kwanza akazaa mwa-
na, akamwita jina lake Moa-
bu.[h] Yeye ndiye baba ya Moabu,
mpaka leo hii.[i] **38** Yule mdo-
go pia akazaa mwana. Akamwi-
ta jina lake Ben-ami. Yeye ndiye
baba ya wana wa Amoni,[j] mpa-
ka leo hii.

SURA 19
a Mwa 19:17
b Mwa 19:22
c Mwa 38:8
d Mwa 9:21
Hab 2:15
e Law 18:6
f 1Th 5:7
g Law 18:7
Eze 22:10
h Kum 2:9
i Ru 2:6
1Nya 18:2
j Kum 2:19
Amu 11:4
Ne 13:1
Sef 2:9

Safu ya 2

SURA 20
a Mwa 13:18
b Hes 13:26
c Mwa 25:18
d Mwa 10:19
e Mwa 12:13
Mwa 20:12
f Mwa 12:15
g Mwa 12:17
Zb 105:14
h Kum 22:22
i Law 18:19
j Mwa 18:25
k 1Nya 29:17
Zb 26:6
l 1Sa 16:7
Met 21:2
Yer 17:10
m Mwa 39:9
n Met 6:29
1Ko 7:1
o Kut 7:1
Zb 105:15
p Kum 9:20
Ayu 42:8
Yak 5:16
1Pe 3:12
q Eze 3:19

20 Sasa Abrahamu akaha-
misha kambi kutoka
huko[a] mpaka nchi ya Negebu
na kuanza kukaa katikati ya
Kadeshi[b] na Shuri[c] na kukaa
akiwa mgeni Gerari.[d] **2** Na
Abrahamu akasema tena ku-
mhusu Sara mke wake: "Yeye
ni dada yangu."[e] Basi Abime-
leki mfalme wa Gerari aka-
tuma watu, akamchukua Sara.[f]
3 Baadaye Mungu akamjia
Abimeleki katika ndoto ya usi-
ku, akamwambia: "Tazama,
wewe ni kama tu umekufa, kwa
sababu ya mwanamke amba-
ye umemchukua,[g] kwa kuwa
yeye ni mke wa mwingine."[h]
4 Hata hivyo, Abimeleki ha-
kuwa amemkaribia.[i] Kwa hiyo
akasema: "Yehova, je, utaua ta-
ifa ambalo kwa kweli ni le-
nye uadilifu?[j] **5** Je, yeye ha-
kuniambia, 'Huyu ni dada ya-
ngu'? naye huyu—je, yeye
pia hakusema, 'Yeye ni ndu-
gu yangu'? Mimi nimefanya ja-
mbo hili katika unyoofu wa
moyo wangu na bila hatia miko-
noni mwangu."[k] **6** Basi Mu-
ngu wa kweli akamwambia ka-
tika ndoto: "Mimi pia nime-
jua kwamba katika unyoofu
wa moyo wako umefanya hili,[l]
nami pia nilikuwa nikikuzu-
ia usinitendee dhambi.[m] Ndi-
yo sababu mimi sikukuruhusu
umguse.[n] **7** Lakini sasa mru-
dishe mke wa huyo mwanamu-
me, kwa maana yeye ni nabii,[o]
naye atakuombea dua.[p] Kwa
hiyo uendelee kuishi. Lakini
ikiwa humrudishi, jua kwamba
utakufa hakika, wewe na wote
walio wako."[q]

8 Kwa hiyo Abimeleki akaa-
mka asubuhi na mapema, aka-
waita watumishi wake wote na

kuyasema mambo hayo yote
masikioni mwao. Na watu hao
wakaogopa sana. **9** Kisha
Abimeleki akamwita Abraha-
mu na kumwambia: "Umetute-
ndea nini, na ni dhambi gani ni-
mekutendea, hata ukaleta juu
yangu na ufalme wangu dha-
mbi kubwa?[a] Matendo ambayo
hayakupaswa kutendwa, wewe
umetenda kuhusiana nami."[b]
10 Na Abimeleki akaendelea
kumwambia Abrahamu: "Uli-
kuwa na lengo gani kwa ku-
fanya jambo hili?"[c] **11** Abra-
hamu akajibu akasema: "Ni
kwa sababu nilisema moyo-
ni mwangu, 'Bila shaka maha-
li hapa hawamwogopi Mungu.[d]
Nao hakika wataniua kwa sa-
babu ya mke wangu.'[e] **12** Na,
tena, yeye kwa kweli ni dada
yangu, ni binti ya baba ya-
ngu, ila tu si binti ya mama ya-
ngu; naye akawa mke wangu.[f]
13 Ikawa kwamba, Mungu ali-
ponihamisha kutoka katika
nyumba ya baba yangu,[g] ndi-
po nilipomwambia yeye, 'Hizi
ni fadhili zenye upendo[h] unazo-
weza kunionyesha: Kila mahali
ambako tutakwenda sema hivi
kunihusu: "Yeye ni ndugu ya-
ngu."'"[i]

14 Basi Abimeleki akachu-
kua kondoo na ng'ombe na wa-
tumishi wanaume na wajaka-
zi, akampa Abrahamu na
kumrudishia mke wake Sara.[j]
15 Tena Abimeleki akasema:
"Tazama, nchi yangu iko
wazi kwako. Kaa mahali amba-
po ni pema machoni pako."[k]
16 Naye akamwambia Sara:
"Tazama, mimi nampa ndugu
yako[l] vipande elfu moja vya
pesa za fedha. Tazama, hizo zi-
takuwa kifuniko[m] cha macho
kwako kwa wote walio pamo-
ja nawe, na mbele ya kila mtu,
nawe umeondolewa shutuma."
17 Naye Abrahamu akaanza
kumwomba dua Mungu wa
kweli;[a] naye Mungu akamponya
Abimeleki na mke wake na vi-
jakazi wake, nao wakaanza ku-
zaa watoto. **18** Kwa maana
Yehova alikuwa amefunga kabi-
sa kila tumbo la uzazi la
nyumba ya Abimeleki kwa sa-
babu ya Sara, mke wa Abra-
hamu.[b]

21 Naye Yehova akamwele-
kezea Sara fikira kama
alivyokuwa amesema, na sasa
Yehova akamtendea Sara kama
alivyokuwa amesema.[c] **2** Naye
Sara akapata mimba,[d] kisha aka-
mzalia Abrahamu mwana katika
umri wake wa uzee kwa wakati
uliowekwa ambao Mungu ali-
kuwa amemwambia.[e] **3** Basi
Abrahamu akamwita mwana
wake jina lake Isaka,[f] aliye-
kuwa amezaliwa kwake, amba-
ye Sara alikuwa amemza-
lia. **4** Naye Abrahamu aka-
mtahiri Isaka mwana wake
akiwa na umri wa siku nane,
kama Mungu alivyokuwa ame-
mwamuru.[g] **5** Naye Abraha-
mu alikuwa na umri wa miaka
mia moja wakati Isaka mwa-
na wake alipozaliwa. **6** Ki-
sha Sara akasema: "Mungu
amenitayarishia kicheko: kila
mtu anayesikia hilo atanicheka."[h]
7 Naye akaongeza ku-
sema: "Ni nani ambaye ange-
mwambia Abrahamu, 'Sara
atanyonyesha watoto,' maana
nimezaa mwana katika umri
wake wa uzee?"

8 Sasa huyo mtoto aka-
endelea kukua, akafikia ku-
achishwa kunyonya;[i] na ki-
sha Abrahamu akatayarisha

SURA 20
a Law 20:10
Ebr 13:4
b Met 28:10
c Mwa 12:18
Mwa 26:10
d Ayu 1:1
Met 8:13
e Mwa 12:12
Mwa 26:7
f Mwa 11:29
g Mwa 12:1
Mdo 7:3
h Mwa 47:29
Ru 3:10
2Sa 9:7
Kol 3:12
i Mwa 12:13
Efe 5:22
j Mwa 12:16
k Mwa 47:6
l Mwa 12:13
Mwa 20:2
m Met 12:16

Safu ya 2
a Met 15:8
Yak 5:16
b Mwa 12:17

SURA 21
c Mwa 18:10
d Ebr 11:11
e Mwa 17:21
Mwa 18:14
2Fa 4:17
Ro 9:9
f Mwa 17:19
Yos 24:3
Ro 9:7
g Mwa 17:12
Law 12:3
Lu 2:21
Yoh 7:22
Mdo 7:8
h Mwa 18:12
i 1Sa 1:22

karamu kubwa katika siku ya
Isaka kuachishwa kunyonya.
9 Na Sara akawa anaona mwa-
na wa Hagari Mmisri,[a] ambaye
alikuwa amemzalia Abrahamu,
akidhihaki.[b] **10** Kwa hiyo
akaanza kumwambia Abraha-
mu: "Mfukuze kijakazi huyu na
mwana wake, kwa maana mwa-
na wa kijakazi huyu hatakuwa
mrithi pamoja na mwanangu,
Isaka!"[c] **11** Lakini jambo
hilo kuhusu mwana wake
halikumpendeza Abrahamu
hata kidogo.[d] **12** Kisha Mungu
akamwambia Abrahamu:
"Usiruhusu jambo lolote amba-
lo Sara anazidi kukuambia liwe
lisilokupendeza juu ya huyo
mvulana na juu ya kijakazi
wako. Sikiliza sauti yake, kwa
sababu ule utakaoitwa uzao
wako utakuwa kupitia Isaka.[e]
13 Nami nitamfanya pia huyo
mwana wa kijakazi[f] kuwa tai-
fa, kwa sababu yeye ni uzao
wako."[g]

14 Basi Abrahamu akaamka
asubuhi na mapema, akachu-
kua mkate na kiriba cha maji
akampa Hagari,[h] akakiweka
juu ya bega lake, na yule mto-
to,[i] halafu akamruhusu aende.
Naye akaenda zake, akatanga-
tanga katika nyika ya Beer-
sheba.[j] **15** Mwishowe yale
maji yakamalizika[k] ndani ya
kiriba, naye akamtupa[l] mto-
to chini ya mti mmoja. **16** Ki-
sha akaenda mbele na kuketi
chini peke yake, kama umba-
li wa mtupo wa upinde, kwa
sababu alisema: "Acha mimi ni-
simwone mtoto anapokufa."[m]
Kwa hiyo akaketi chini umba-
li fulani akaanza kupaaza sau-
ti na kulia.[n]

17 Ndipo Mungu akaisikia
sauti ya huyo mvulana,[o] na

SURA 21

a Mwa 16:4
b Mwa 15:13
Mdo 7:6
Ga 4:29
c Mwa 15:4
Yoh 8:35
Ga 4:30
d Mwa 17:18
e Mwa 17:19
Ro 9:7
Ebr 11:18
f Ga 4:22
g Mwa 16:10
Mwa 17:20
Mwa 25:12
h Zb 119:60
i Mwa 25:6
j Mwa 22:19
k Kut 15:22
Kut 17:3
Zb 63:1
l Mt 15:30
m Est 8:6
Isa 49:15
n Zek 12:10
Lu 7:13
o Mwa 16:11
Zb 22:24
Zb 68:5
Zb 146:9

Safu ya 2

a Mwa 16:7
b 1Nya 1:29
c 2Fa 6:17
d Mwa 16:16
Mwa 21:5
e Mwa 27:3
f Hes 10:12
g Mwa 20:17
Mwa 26:28
Ro 8:31
1Ko 14:25
h Kum 6:13
i Yos 2:12
1Sa 20:42
Yer 4:2
j Mwa 24:14
k Mwa 20:15
Mwa 26:3
l Mwa 14:22
Ebr 6:16
m Mwa 26:15
Mwa 26:20
Kut 2:17

malaika wa Mungu akamwi-
ta Hagari kutoka mbinguni na
kumwambia:[a] "Una nini, Haga-
ri? Usiogope, kwa sababu Mu-
ngu amesikiliza sauti ya huyo
mvulana pale alipo. **18** Si-
mama, mwinue huyo mvula-
na, umshike kwa mkono wako,
kwa sababu nitamfanya kuwa
taifa kubwa."[b] **19** Kisha Mu-
ngu akafungua macho yake
hata akaona kisima cha maji,[c]
naye akaenda, akaanza kuki-
jaza maji kiriba na kumnywe-
sha huyo mvulana. **20** Na
Mungu akaendelea kuwa na
huyo mvulana,[d] naye akaende-
lea kukua na kukaa nyikani;
naye akawa mpiga-mishale.[e]
21 Naye akakaa katika nyika
ya Parani,[f] na mama yake aka-
mchukulia mke kutoka nchi ya
Misri.

22 Sasa ikawa wakati huo
kwamba Abimeleki pamoja na
Fikoli mkuu wa jeshi lake wa-
kamwambia Abrahamu: "Mu-
ngu yuko pamoja nawe ka-
tika kila jambo unalofanya.[g]
23 Basi sasa niapie hapa kwa
Mungu[h] kwamba hutanitendea
kwa udanganyifu mimi na wa-
toto wangu na wazao wangu;[i]
kwamba, kulingana na upendo
mshikamanifu ambao nimeku-
tendea,[j] utanitendea mimi na
nchi ambayo katika hiyo ume-
kuwa ukikaa ukiwa mgeni."[k]
24 Kwa hiyo Abrahamu akase-
ma: "Nitaapa."[l]

25 Abrahamu alipomlaumu
vikali Abimeleki kwa haba-
ri ya kisima cha maji ambacho
watumishi wa Abimeleki wali-
kuwa wamechukua kwa jeu-
ri,[m] **26** ndipo Abimeleki aka-
sema: "Mimi sijui ni nani ali-
yefanya jambo hili, wala wewe
mwenyewe hukuniambia hilo,

wala mimi mwenyewe pia sijasikia hilo ila leo tu."[a] **27** Basi
Abrahamu akachukua kondoo na ng'ombe akampa Abimeleki,[b] na wote wawili wakafanya agano.[c] **28** Abraham-
u alipoweka kando wana-kondoo jike saba wa kundi,
29 Abimeleki akamwambia
Abrahamu: "Hapa inamaanisha nini hawa wana-kondoo
jike saba ambao umewaweka peke yao?" **30** Kisha akasema: "Wewe utakubali mkononi mwangu hao wana-kondoo
jike saba kuwa ushahidi[d] kwangu kwamba nimechimba kisima hiki." **31** Hiyo ndiyo sababu aliita mahali hapo Beer-
sheba,[e] kwa sababu wote wawili walikuwa wamekula kiapo
hapo. **32** Kwa hiyo wakafanya agano[f] huko Beer-sheba,
halafu Abimeleki akaisimama pamoja na Fikoli mkuu wa jeshi lake nao wakarudi mpaka
nchi ya Wafilisti.[g] **33** Kisha akapanda mkwaju huko Beer-
sheba naye akaliitia hapo jina la Yehova,[h] Mungu anayedumu mpaka wakati usio na kipimo.[i] **34** Naye Abrahamu akaendelea kukaa siku nyingi akiwa mgeni katika nchi ya Wafilisti.[j]

22 Baada ya mambo hayo
Mungu wa kweli akamjaribu Abrahamu.[k] Kwa hiyo
akamwambia: "Abrahamu!"
naye akajibu, akasema: "Mimi hapa!"[l] **2** Naye akaendelea
kusema: "Tafadhali, mchukue mwana wako, mwana wako wa pekee unayempenda sana,[m]
Isaka,[n] ufunge safari kwenda nchi ya Moria[o] na huko umtoe kama toleo la kuteketezwa juu
ya mmoja kati ya milima ambao nitakuonyesha."[p]

SURA 21
a 2Ko 7:11
b Mwa 33:11
Met 17:8
c Mwa 26:28
1Sa 18:3
Ga 3:15
d Mwa 31:52
e Mwa 26:33
f Mwa 26:28
g Mwa 10:14
Mwa 26:1
Kut 13:17
h Mwa 12:8
Mwa 26:25
i Zb 90:2
Isa 40:28
Yer 10:10
1Ti 1:17
j Ebr 11:9

SURA 22
k Ayu 1:12
Ebr 4:15
Ebr 5:8
1Pe 1:7
l Isa 6:8
m Met 4:3
Met 8:30
Yoh 3:16
Yoh 10:17
n Mwa 17:19
Yos 24:3
Ro 9:7
o 2Nya 3:1
p Kum 12:14

Safu ya 2
a Mwa 26:5
Zb 119:60
b Mwa 12:16
c Zb 95:6
Mt 4:10
d Yoh 19:17
e Isa 53:7
1Pe 2:23
f Mt 26:39
Ro 8:15
g Isa 58:9
Yoh 8:29
h Kut 12:5
Ro 8:36
i Yoh 1:29
Efe 5:2
Ebr 10:5
1Pe 1:19
j Mwa 12:7
Kut 20:25
Ebr 13:10

3 Kwa hiyo Abrahamu akaamka asubuhi na mapema na kumtandika punda wake, akachukua wawili kati ya watumishi
wake na Isaka mwana wake;[a]
naye akapasua kuni kwa ajili ya toleo la kuteketezwa. Kisha akaondoka, akafunga safari kwenda mahali ambapo Mungu wa kweli alimwonyesha.
4 Ilikuwa kwanza katika siku ya tatu kwamba Abrahamu alinua macho yake akaanza kupaona mahali hapo kwa mbali. **5** Sasa Abrahamu akawaambia watumishi wake:[b] "Ninyi
kaeni hapa pamoja na punda, lakini mimi na huyu mvulana tunataka kwenda mbele huko tukaabudu,[c] halafu tutarudi hapa
mlipo."

6 Baada ya hayo Abrahamu alichukua kuni za toleo la kuteketezwa akamtwika Isaka
mwana wake,[d] naye akachukua mikononi mwake moto na kisu cha kuchinjia, na wote wawili wakasonga mbele pamoja.[e]
7 Na Isaka akaanza kumwambia Abrahamu baba yake:
"Baba yangu!"[f] Naye akasema:
"Mimi hapa, mwanangu!"[g] Basi akaendelea kusema: "Hapa
pana moto na kuni, lakini yuko wapi kondoo kwa ajili ya toleo la kuteketezwa?"[h] **8** Abraham-
u akajibu akasema: "Mungu mwenyewe ataandaa kondoo wa toleo la kuteketezwa,[i] mwanangu." Na wote wawili wakaendelea kutembea pamoja.

9 Mwishowe wakafika mahali ambapo Mungu wa kweli alikuwa amemwonyesha, naye
Abrahamu akajenga madhabahu[j] hapo na kuziweka kuni
kwa utaratibu, akamfunga Isaka mwana wake mikono na miguu na kumweka juu ya madhabahu

juu ya zile kuni.[a] **10** Kisha
Abrahamu akanyoosha mkono
wake akachukua kile kisu cha
kuchinjia ili amuue mwana
wake.[b] **11** Lakini malaika wa
Yehova akaanza kumwita ku-
toka mbinguni akisema:[c] "Abra-
hamu, Abrahamu!" naye akaji-
bu: "Mimi hapa!" **12** Naye aka-
endelea kusema: "Usinyooshe
mkono wako juu ya huyo mvu-
lana wala usimtendee jambo lo-
lote kamwe,[d] kwa maana sasa
mimi najua kwamba wewe una-
mwogopa Mungu kwa kuwa hu-
kunizuilia mwana wako, mwa-
na wako wa pekee."[e] **13** Kisha
Abrahamu akainua macho yake,
akatazama na kumbe, kule mbe-
le, kulikuwa na kondoo-dume
aliyenaswa kwa pembe zake ki-
chakani. Kwa hiyo Abrahamu
akaenda, akamchukua huyo ko-
ndoo-dume, akamtoa kuwa to-
leo la kuteketezwa badala ya
mwana wake.[f] **14** Naye Abra-
hamu akaanza kuita jina la ma-
hali hapo Yehova-yire. Ndiyo
sababu leo kwa desturi huse-
mwa: "Katika mlima wa Yehova
itaandaliwa."[g]

15 Na malaika wa Yehova
akamwita Abrahamu mara ya
pili kutoka mbinguni **16** aka-
mwambia: "'Naapa kwa nafsi
yangu mwenyewe,' asema Ye-
hova,[h] 'kwamba kwa sababu
ya uhakika wa kwamba wewe
umefanya jambo hili nawe hu-
kuzuia mwana wako, mwana
wako wa pekee,[i] **17** hakika
nitakubariki nami nitauzidi-
sha uzao wako kama nyota za
mbinguni na kama chembe za
mchanga zilizo kando ya ba-
hari;[j] na uzao wako utamili-
ki lango la adui zake.[k] **18** Na
kupitia kwa uzao wako[l] mataifa yote ya dunia hakika yataji-
bariki kwa sababu wewe umei-
sikiliza sauti yangu.'"[a]

19 Baada ya hayo Abraha-
mu akarudi kwa watumishi
wake, nao wakasimama, waka-
enda pamoja mpaka Beer-she-
ba.[b] Abrahamu akaendelea ku-
kaa Beer-sheba.

20 Basi ikawa kwamba baa-
da ya mambo hayo habari ika-
mfikia Abrahamu: "Tazama,
Milka[c] pia amemzalia Naho-
ri[d] ndugu yako wana: **21** Usi
mzaliwa wake wa kwanza na
Buzi[e] ndugu yake na Kemueli
baba ya Aramu, **22** na Kese-
di na Hazo na Pildashi na Yi-
dlafu na Bethueli."[f] **23** Naye
Bethueli akamzaa Rebeka.[g]
Hao wanane Milka alimzalia
Nahori ndugu ya Abrahamu.
24 Kulikuwa na suria wake
pia, ambaye jina lake lilikuwa
Reuma. Baada ya muda yeye
pia akazaa Teba na Gahamu na
Tahashi na Maaka.[h]

23 Na maisha ya Sara yaka-
wa miaka 127. Hiyo ndi-
yo iliyokuwa miaka ya maisha
ya Sara.[i] **2** Basi Sara aka-
fa katika Kiriath-arba,[j] yaani,
Hebroni[k] katika nchi ya Kana-
ani,[l] naye Abrahamu akaingia
ndani kumwombolezea Sara na
kumlilia. **3** Kisha Abrahamu
akaondoka mbele ya mfu wake
akaanza kuongea na wana wa
Hethi,[m] akisema: **4** "Mimi ni
mkaaji na mhamiaji katikati
yenu.[n] Nipeni mahali pangu pa
kuzikia katikati yenu ili niwe-
ze kumzika mfu wangu kuto-
ka machoni pangu."[o] **5** Basi
wana wa Hethi wakamjibu
Abrahamu, na kumwambia:
6 "Tusikilize, bwana wangu.[p]
Wewe ni mkuu katikati yetu,
mtu wa Mungu.[q] Katika mahali

SURA 22
a Mt 27:2
Yoh 10:18
Mdo 8:32
Flp 2:8
b Mt 10:37
Ro 8:32
Ebr 2:18
Ebr 11:17
Yak 2:21
c Zb 34:7
Zb 91:11
Mt 17:5
d Zb 34:20
Yoh 19:36
e Mwa 26:5
Ebr 11:19
Yak 2:21
1Yo 4:10
1Yo 5:3
f Law 16:3
g Mwa 22:2
2Nya 3:1
Isa 25:6
h Zb 105:9
Isa 45:23
Ebr 6:13
i Yoh 3:16
Ro 8:32
Ebr 11:17
j Mwa 13:16
Mwa 15:5
Mdo 3:25
Ga 3:29
Ebr 6:14
k 2Sa 11:23
Zb 2:8
Da 2:44
Ebr 2:14
Ufu 11:15
l Mwa 3:15
Ro 9:7
Ga 3:16

Safu ya 2
a Zek 8:23
Ga 3:8
b Mwa 21:31
c Mwa 11:29
d Mwa 11:26
e Ayu 32:2
f Mwa 25:20
g Mwa 24:15
Ro 9:10
h 2Sa 10:6

SURA 23
i Mwa 17:17
j Yos 14:15
k Mwa 35:27
Hes 13:22
l Mwa 12:5
Zb 105:11
m Mwa 10:15
Mwa 23:20
n Mwa 17:8
Ebr 11:9
o Mwa 49:30
Mdo 7:5
p Mwa 43:20
q Mwa 21:22

petu palipo bora kabisa pa kuzikia, zika mfu wako.[a] Hakuna yeyote kati yetu atakayekunyima mahali pake pa kuzikia ili usizike mfu wako."[b]

7 Basi Abrahamu akasimama, akawainamia hao wenyeji,[c] wana wa Hethi,[d] **8** na kuongea nao akisema: "Ikiwa nafsi zenu zinakubali kuzika mfu wangu kutoka machoni pangu, nisikilizeni na kumhimiza Efroni mwana wa Zohari kwa ajili yangu,[e] **9** kwamba apate kunipa pango la Makpela,[f] ambalo ni lake, lililo mwisho wa shamba lake. Na anipe hilo kati yenu kwa kiwango kamili cha fedha liwe mahali pangu pa kuzikia."[g]

10 Basi, Efroni alikuwa amekaa kati ya wana wa Hethi. Kwa hiyo Efroni Mhiti[h] akamjibu Abrahamu masikioni mwa wana wa Hethi pamoja na wale wote waliokuwa wakiingia lango la jiji, akisema:[i] **11** "Hapana, bwana wangu! Nisikilize. Hilo shamba mimi nakupa wewe, na lile pango lililomo nakupa. Mbele ya macho ya wana wa watu wangu nakupa.[j] Zika mfu wako." **12** Kisha Abrahamu akainama mbele ya hao wenyeji **13** na kuongea na Efroni masikioni mwa hao wenyeji, akisema: "Laiti wewe —hapana, nisikilize! Mimi nitakupa kiwango cha fedha kwa ajili ya shamba hilo. Kichukue kutoka kwangu,[k] ili nipate kumzika mfu wangu hapo."

14 Kisha Efroni akamjibu Abrahamu, akimwambia hivi: **15** "Bwana wangu, nisikilize. Sehemu ya shamba yenye thamani ya shekeli za fedha mia nne, hiyo ni nini kati yangu na wewe? Kwa hiyo zika mfu wako."[a] **16** Naye Abrahamu akamsikiliza Efroni, na Abrahamu akampimia Efroni hicho kiwango cha fedha alichokuwa amesema masikioni mwa wana wa Hethi, shekeli za fedha mia nne zinazotumiwa na wanabiashara.[b] **17** Kwa hiyo shamba la Efroni lililokuwa Makpela, iliyo mbele ya Mamre, lile shamba na lile pango lililokuwamo na miti yote iliyokuwa shambani,[c] iliyokuwa ndani ya mipaka yake yote kuzunguka, ikathibitishiwa[d] **18** Abrahamu kuwa mali yake iliyonunuliwa mbele ya macho ya wana wa Hethi kati ya wale wote wanaoingia katika lango la jiji lake.[e] **19** Na baada ya hayo Abrahamu akamzika Sara mke wake katika pango la shamba la Makpela mbele ya Mamre, yaani, Hebroni, katika nchi ya Kanaani.[f] **20** Hivyo lile shamba na lile pango lililokuwamo likathibitishiwa Abrahamu kuwa mahali pake pa kuzikia mikononi mwa wana wa Hethi.[g]

24 Abrahamu alikuwa mzee, amesonga katika miaka; na Yehova alikuwa amembariki Abrahamu katika kila jambo.[h] **2** Kwa hiyo Abrahamu akamwambia mtumishi wake, yule mwenye umri mkubwa zaidi wa nyumbani mwake, aliyekuwa anasimamia vyote alivyokuwa navyo:[i] "Tafadhali, weka mkono wako chini ya paja langu,[j] **3** kwa kuwa lazima nikuapishe kwa Yehova,[k] Mungu wa mbingu na Mungu wa dunia, kwamba hutamchukulia mwanangu mke kutoka kwa binti za Wakanaani ambao ninakaa kati yao,[l] **4** bali utaenda mpaka nchi yangu na mpaka

SURA 23
a Isa 53:9
Yoh 19:41
b Yos 24:32
c 1Pe 2:17
d 1Nya 1:13
e Mwa 25:9
f Mwa 49:30
g Mwa 23:15
h Mwa 50:13
i Mwa 34:20
Kum 16:18
Ru 4:1
j Kum 19:15
Ru 4:4
k Mwa 14:23
Ro 13:8

Safu ya 2
a 2Sa 2:5
b Ezr 8:25
Mdo 7:16
c Mwa 25:9
Mwa 49:30
d Ru 4:11
Yer 32:44
e Ayu 29:7
Yer 32:12
f Mwa 25:10
Mwa 50:13
g Mwa 49:31
Mdo 7:5

SURA 24
h Mwa 13:2
Ga 3:9
i Mwa 15:2
Mwa 41:40
1Ko 4:2
j Mwa 47:29
k Mwa 21:23
l Mwa 28:1
Kum 7:3
1Ko 7:39
2Ko 6:14

kwa watu wa jamaa yangu,[a]
nawe utamchukulia mwana-
ngu, Isaka, mke."
5 Lakini, huyo mtumishi
akamwambia: "Itakuwaje iki-
wa mwanamke huyo hata-
ki kuja pamoja nami mpaka
nchi hii? Je, ni lazima niha-
kikishe kwamba nimemru-
disha mwana wako mpaka
nchi ambayo wewe ulitoka?"[b]
6 Abrahamu akajibu akamwa-
mbia: "Jihadhari usimrudishe
mwanangu huko.[c] **7** Yehova
Mungu wa mbingu, aliyenichu-
kua kutoka katika nyumba ya
baba yangu na kutoka kati-
ka nchi ya watu wa jamaa ya-
ngu[d] na ambaye alisema nami
na ambaye aliniapia,[e] akise-
ma, 'Nitaupa uzao wako[f] nchi
hii,'[g] atatuma malaika wake
mbele yako,[h] nawe utachukua
mke huko kwa ajili ya mwa-
nangu.[i] **8** Lakini ikiwa huyo
mwanamke hataki kuja pa-
moja nawe, wewe pia utaku-
wa umewekwa huru kutoka
kwenye kiapo hiki ulichonipa.[j]
Ila tu usimrudishe mwanangu
huko." **9** Basi huyo mtumishi
akaweka mkono wake chini ya
paja la Abrahamu bwana wake
na kumwapia kuhusu jambo
hilo.[k]
10 Basi huyo mtumishi aka-
chukua ngamia kumi kutoka
kwa ngamia za bwana wake,
akatoka kwenda na kila namna
ya kitu chema cha bwana wake
mkononi mwake.[l] Kisha akao-
ndoka na kwenda Mesopota-
mia mpaka katika jiji la Na-
hori. **11** Mwishowe akafanya
wale ngamia wapige magoti
chini nje ya jiji kwenye kisima
cha maji karibu na wakati wa
jioni,[m] karibu na wakati ambao
wanawake wanaoteka maji wa-

SURA 24
a Mwa 22:20
b Mwa 11:28
Mwa 15:7
c Ebr 11:15
d Mwa 12:1
Ebr 11:8
e Mik 7:20
Lu 1:73
Ebr 6:13
f Mwa 26:4
Mdo 7:5
Ebr 11:18
g Mwa 13:15
Kut 32:13
Kum 34:4
h Kut 23:20
Zb 34:7
Ebr 1:14
i Mwa 12:5
Mdo 7:4
j Yos 2:17
k Mwa 24:2
Mwa 47:29
l Mwa 24:35
Mwa 43:11
m Met 12:10

Safu ya 2
a Kut 2:16
1Sa 9:11
Yoh 4:7
b Mwa 32:9
1Fa 18:36
Mt 22:32
c Ne 1:11
Zb 37:5
Flp 4:6
d 1Sa 20:8
Zek 7:9
e Mwa 29:10
f Met 19:14
g Amu 6:17
Amu 18:5
h Zb 34:15
Zb 65:2
Isa 58:9
Isa 65:24
1Yo 5:14
i Mwa 22:23
j Mwa 11:29
k Mwa 11:26
l Mwa 21:14
m Mwa 26:7
n Kum 22:20
2Ko 11:2
o Yoh 4:7
p Mt 10:42
Mt 25:35

likuwa na desturi ya kutoka
nje.[a] **12** Naye akaendelea ku-
sema: "Yehova Mungu wa bwa-
na wangu Abrahamu,[b] tafa-
dhali, fanya hilo litukie mbe-
le yangu leo nawe umfanyie
bwana wangu Abrahamu[c] fa-
dhili zenye upendo.[d] **13** Hapa
nimesimama kwenye chemche-
mi ya maji, na binti za watu wa
jiji wanatoka nje kuteka maji.[e]
14 Litakalotokea ni kwamba
mwanamke kijana ambaye ni-
tamwambia, 'Tafadhali, shu-
sha mtungi wako wa maji ili
ninywe,' na ambaye kwa kwe-
li atasema, 'Kunywa, na pia ni-
tanywesha ngamia zako,' huyo
ndiye utakayemchagulia mtu-
mishi wako,[f] Isaka; na kwa
hilo unijulishe kwamba umefa-
nya upendo mshikamanifu kwa
bwana wangu."[g]
15 Basi, ikawa kwamba ka-
bla hajamaliza kusema,[h] taza-
ma, Rebeka, aliyezaliwa na Be-
thueli[i] mwana wa Milka[j] mke
wa Nahori,[k] ndugu ya Abra-
hamu, alikuwa akitoka nje na
mtungi wake wa maji ukiwa
begani mwake.[l] **16** Sasa huyo
mwanamke kijana alikuwa
mwenye sura ya kuvutia sana,[m]
bikira, wala hakuna mwana-
mume aliyekuwa amelala
naye.[n] Akateremka kuja kwe-
nye chemchemi, akaanza ku-
jaza mtungi wake wa maji ki-
sha akapanda. **17** Mara moja
yule mtumishi akakimbia aku-
tane naye na kusema: "Tafa-
dhali, nipe maji kidogo kati-
ka mtungi wako."[o] **18** Naye
akasema: "Kunywa, bwana wa-
ngu." Kisha akashusha upesi
mtungi wake mkononi mwake,
akamnywesha.[p] **19** Alipoku-
wa amemaliza kumnywesha,
akasema: "Nitateka maji pia

kwa ajili ya ngamia zako
mpaka wamalize kunywa."[a]
20 Kwa hiyo akamimina upesi
maji ya mtungi wake ndani ya
chombo cha kunyweshea wa-
nyama naye akakimbia tena na
tena kisimani ili kuteka maji,[b]
akaendelea kuteka kwa ajili
ya ngamia zake wote. **21** Wa-
kati huo wote yule mwanamu-
me alikuwa anamkazia macho
kwa kustaajabu, akikaa kimya
ili ajue ikiwa Yehova alikuwa
amefanikisha safari yake au si-
vyo.[c]
22 Basi ikawa kwamba, wa-
kati hao ngamia walipoku-
wa wamemaliza kunywa, yule
mwanamume akachukua pete
ya puani[d] ya dhahabu yenye
uzito wa nusu shekeli na vi-
kuku[e] viwili kwa ajili ya mi-
kono yake, uzito wake uliku-
wa shekeli kumi za dhahabu,
23 naye akasema: "Wewe ni bi-
nti ya nani? Tafadhali niambie.
Je, mna nafasi yoyote nyumba-
ni kwa baba yako tukae usiku
huu?"[f] **24** Akajibu akamwa-
mbia: "Mimi ni binti ya Bethu-
eli[g] mwana wa Milka, ambaye
alimzalia Nahori."[h] **25** Naye
akamwambia tena: "Tuna ma-
jani na chakula kingi cha mi-
fugo, pia mahali pa kukaa usi-
ku."[i] **26** Ndipo huyo mwana-
mume akainama chini akajila-
za kifudifudi mbele za Yehova[j]
27 na kusema: "Abarikiwe Ye-
hova[k] Mungu wa bwana wangu
Abrahamu, ambaye hakuacha
fadhili zake zenye upendo na
kuwa mwenye kutegemeka ku-
mwelekea bwana wangu. Mimi
nikiwa njiani, Yehova ameni-
ongoza kwenye nyumba ya ndu-
gu za bwana wangu."[l]
28 Na yule mwanamke ki-
jana akaenda mbio, akaambia

SURA 24
a Ro 12:13
1Pe 4:9
b Met 31:17
Met 31:31
c Zb 107:43
d Eze 16:12
e Yer 2:32
Eze 16:11
f Mwa 19:2
Amu 19:21
g Mwa 22:23
h Mwa 11:29
i Mwa 18:4
Mwa 19:3
Mwa 43:24
j 1Nya 29:20
Ne 8:6
Zb 95:6
k Mwa 9:26
Zb 72:18
Lu 1:68
l Zb 100:5
Mik 7:20

Safu ya 2
a Mwa 25:20
Mwa 29:10
b Isa 3:21
Yer 2:32
Eze 16:11
c Mwa 26:29
Ru 3:10
Zb 115:15
d Amu 19:21
Lu 7:44
1Ti 5:10
e Ro 12:11
Efe 6:5
f Mwa 15:2
g Mwa 13:2
Zb 107:38

nyumba ya mama yake juu ya
mambo hayo. **29** Sasa Rebe-
ka alikuwa na ndugu na jina
lake lilikuwa Labani.[a] Basi La-
bani akaenda mbio kwa yule
mwanamume aliyekuwa nje
kwenye chemchemi. **30** Ika-
wa kwamba alipoona ile pete
ya puani na vikuku[b] mikono-
ni mwa dada yake na aliposi-
kia maneno ya Rebeka dada
yake, akisema: "Hivi ndivyo
huyo mwanamume alivyose-
ma nami," ndipo akaja kwa
huyo mwanamume na tazama
alikuwa hapo, amesimama ka-
ndo ya ngamia kwenye che-
mchemi. **31** Mara moja aka-
sema: "Njoo, wewe mbarikiwa
wa Yehova.[c] Kwa nini unaende-
lea kusimama hapa nje, waka-
ti mimi mwenyewe nimetayari-
sha nyumba na nafasi kwa aji-
li ya ngamia?" **32** Baada ya
hayo, huyo mwanamume akai-
ngia ndani ya nyumba, naye
akaanza kufungua ngamia lija-
mu na kuwapa ngamia majani
na chakula cha mifugo na maji
ya kuosha miguu yake na mi-
guu ya wanaume waliokuwa
pamoja naye.[d] **33** Kisha cha-
kula kikawekwa mbele yake,
lakini yeye akasema: "Mimi si-
takula mpaka nitakapokuwa
nimesema mambo yangu." Kwa
hiyo akamwambia: "Sema!"[e]
34 Kisha akaendelea ku-
sema: "Mimi ni mtumishi
wa Abrahamu.[f] **35** Na Yeho-
va amembariki bwana wangu
sana kwa kuwa anaendelea
kumfanya mkuu zaidi na ku-
mpa kondoo na ng'ombe na fe-
dha na dhahabu na watumi-
shi wanaume na wajakazi na
ngamia na punda.[g] **36** Tena,
Sara, mke wa bwana wangu ali-
mzalia bwana wangu mwana

baada ya kuzeeka;[a] naye atampa kila kitu alicho nacho.[b]
37 Kwa hiyo bwana wangu aliniapisha, akisema, 'Usimchukulie mwanangu mke kutoka kwa binti za Wakanaani ambao ninakaa katika nchi yao.[c] **38** Sivyo, bali utaenda kwenye nyumba ya baba yangu na kwa familia yangu[d] nawe umchukulie mwanangu mke.'[e] **39** Lakini nikamwambia bwana wangu, 'Itakuwaje ikiwa mwanamke huyo hatakuja pamoja nami?'[f] **40** Kisha akaniambia, 'Yehova, ambaye mbele zake nimetembea,[g] atatuma malaika[h] wake pamoja nawe na kwa hakika atafanikisha njia yako;[i] nawe umchukulie mwanangu mke kutoka kwa familia yangu na kutoka kwa nyumba ya baba yangu.[j]
41 Wakati huo ndipo utakapoondolewa wajibu kwangu kwa kiapo unapofika kwa familia yangu, na ikiwa hawakupi mke, utakuwa bila wajibu kwangu kwa kiapo.'[k]

42 "Nilipofika kwenye chemchemi leo, ndipo nikasema, 'Yehova Mungu wa bwana wangu Abrahamu, ikiwa kwa kweli unafanikisha njia yangu ninayoiendea,[l] **43** hapa mimi nimesimama kwenye chemchemi ya maji. Linalopaswa kutokea ni kwamba mwanamwali[m] anayekuja nje kuteka maji ambaye kwa kweli nitamwambia: "Tafadhali, acha ninywe maji kidogo katika mtungi wako," **44** na ambaye kwa kweli ataniambia: "Unywe wewe, nami pia nitateka maji kwa ajili ya ngamia zako," yeye ndiye mwanamke ambaye Yehova amemchagulia mwana wa bwana wangu.'[n]

SURA 24

a Mwa 21:1
Ro 4:19
Ebr 11:11
b Mwa 25:5
c Mwa 24:3
Mwa 28:1
Ezr 9:2
1Ko 7:39
d Mwa 22:20
e Mwa 24:4
f Mwa 24:5
g Mwa 48:15
1Fa 2:3
Zb 119:3
Isa 38:3
Mdo 9:31
h Kut 23:20
Ebr 1:14
i Mwa 39:3
Ne 1:11
Zb 118:25
j Mwa 11:25
k Mwa 24:9
Yos 2:17
l Zb 37:5
m Mwa 24:16
n Mwa 24:14
Met 18:22
Met 19:14

Safu ya 2

a Zb 65:2
Isa 58:9
Isa 65:24
Da 9:21
b 1Sa 1:13
Ne 2:4
c Mwa 24:15
d Mwa 24:17
e Mwa 24:18
f Mwa 24:23
g Mwa 24:22
Eze 16:11
h Mwa 24:27
Lu 1:68
i Isa 30:21
Isa 48:17
j Mwa 32:10
Mwa 47:29
Yos 2:14
k Mwa 24:8
l Zb 118:23
Mk 12:11
m Mwa 31:24
Isa 46:10
Mdo 5:39
n Met 18:22
Met 19:14

45 "Kabla sijamaliza kusema[a] moyoni[b] mwangu, tazama, Rebeka akatokea, pamoja na mtungi wake juu ya bega lake; naye akateremka mpaka kwenye chemchemi na kuanza kuteka maji.[c] Ndipo nikamwambia, 'Tafadhali, nipe maji.'[d]
46 Kwa hiyo upesi akashusha mtungi wake kutoka kwake, akasema: 'Kunywa,[e] na pia nitanywesha ngamia zako.' Kisha nikanywa, na pia akawanywesha ngamia. **47** Baada ya hayo nikamuuliza na kusema, 'Wewe ni binti ya nani?'[f] naye akasema, 'Mimi ni binti ya Bethueli mwana wa Nahori, ambaye Milka alimzalia.' Ndipo nikaweka pete katika pua yake na vikuku mikononi mwake.[g] **48** Nami nikainama chini na kujilaza kifudifudi mbele za Yehova, nikambariki Yehova, Mungu wa bwana wangu Abrahamu,[h] aliyekuwa ameniongoza katika njia ya kweli[i] ili kuchukua binti ya ndugu ya bwana wangu kwa ajili ya mwana wake. **49** Na sasa ikiwa ninyi kwa kweli mnaonyesha fadhili zenye upendo na kuwa wenye kutegemeka kuelekea bwana wangu,[j] niambieni; lakini ikiwa sivyo, niambieni, ili nipate kugeukia mkono wa kuume au wa kushoto."[k]

50 Ndipo Labani na Bethueli wakajibu na kusema: "Jambo hili limetoka kwa Yehova.[l] Sisi hatuwezi kukuambia baya wala jema.[m] **51** Rebeka huyu mbele yako. Mchukue uende, na awe mke wa mwana wa bwana wako, kama vile ambavyo Yehova amesema."[n] **52** Ikawa kwamba mtumishi wa Abrahamu alipokuwa amesikia maneno yao, mara moja akajilaza ki-

fudifudi chini mbele za Yehova.[a]
53 Na huyo mtumishi akaanza
kutoa vyombo vya fedha na vyo-
mbo vya dhahabu na mavazi
akampa Rebeka; naye akawapa
vitu bora ndugu yake na mama
yake.[b] **54** Baada ya hayo wa-
kala na kunywa, yeye pamo-
ja na wale wanaume waliokuwa
pamoja naye, nao wakakaa
hapo usiku huo, wakaamka asu-
buhi.
Kisha akasema: "Mniache
niende kwa bwana wangu."[c]
55 Na ndugu yake na mama
yake wakajibu wakasema:
"Acha huyu mwanamke ki-
jana akae pamoja nasi anga-
lau kwa siku kumi. Baadaye
anaweza kwenda." **56** Lakini
yeye akawaambia: "Msinizuilie,
kwa kuwa Yehova amefaniki-
sha njia yangu.[d] Acheni niende,
ili nipate kwenda kwa bwana
wangu."[e] **57** Kwa hiyo waka-
sema: "Na tumwite huyo mwa-
namke kijana tusikie kuto-
ka kinywani mwake."[f] **58** Ki-
sha wakamwita Rebeka na ku-
mwambia: "Je, wewe utaenda
na mwanamume huyu?" Naye
akasema: "Mimi niko tayari
kwenda."[g]
59 Basi wakamuaga Rebe-
ka[h] dada yao aende na mtu-
nzaji wake[i] na mtumishi wa
Abrahamu na wanaume wake.
60 Nao wakaanza kumbariki
Rebeka na kumwambia: "Ewe
dada yetu, na uwe maelfu mara
elfu kumi, na uzao wako na
umiliki lango la wale wanao-
uchukia."[j] **61** Baada ya hayo
Rebeka na watumishi wake wa-
nawake[k] wakaondoka wakae-
nda wakiwa wamepanda juu
ya ngamia,[l] wakimfuata yule
mwanamume; na huyo mtumi-
shi akamchukua Rebeka akae-
nda zake.
62 Sasa Isaka alikuwa ame-
kuja kutoka njia inayoenda
Beer-lahai-roi,[a] kwa maana ali-
kuwa anakaa katika nchi ya
Negebu.[b] **63** Na Isaka aliku-
wa nje akitembea ili atafaka-
ri[c] shambani karibu na wakati
wa jioni. Alipoinua macho yake
na kutazama, kumbe, kule nga-
mia walikuwa wakija! **64** Re-
beka alipoinua macho yake,
akamwona Isaka, naye akaru-
ka chini kutoka kwenye nga-
mia. **65** Kisha akamwambia
yule mtumishi: "Yule mwa-
namume anayetembea pale
shambani kuja kutupokea, ni
nani?" naye mtumishi akase-
ma: "Ni bwana wangu." Naye
Rebeka akachukua kitambaa
cha kichwani, akajifunika.[d]
66 Na yule mtumishi akaanza
kumsimulia Isaka mambo yote
aliyokuwa amefanya. **67** Ba-
ada ya hayo Isaka akamleta Re-
beka ndani ya hema la Sara
mama yake.[e] Hivyo akamchu-
kua Rebeka, naye akawa mke
wake;[f] naye akampenda,[g] na
Isaka akapata faraja baada ya
kumpoteza mama yake.[h]

25 Kisha, kwa mara nyingi-
ne Abrahamu akachu-
kua mke, naye aliitwa jina lake
Ketura.[i] **2** Baada ya muda
akamzalia Zimrani na Yoksha-
ni na Medani na Midiani[j] na
Ishbaki na Shua.[k]
3 Yokshani akamzaa She-
ba[l] na Dedani.[m]
Na wana wa Dedani waka-
wa Ashurimu na Letushimu
na Leumimu.
4 Na wana wa Midiani wa-
likuwa Efa[n] na Eferi na Hano-
ki na Abida na Eldaa.[o]

SURA 24
a 1Nya 29:20
2Nya 20:18
b Mwa 34:12
c Mwa 30:25
Mwa 31:27
d Mwa 39:3
Zb 1:3
Isa 48:15
e Zb 123:2
Kol 3:22
1Pe 2:18
f Yoh 9:21
g Mwa 2:24
Zb 45:10
h Mwa 28:5
i Mwa 35:8
j Mwa 22:17
2Sa 12:29
k Zb 45:14
l Mwa 31:17
Mwa 31:34

Safu ya 2
a Mwa 16:14
Mwa 25:11
b Mwa 12:9
Mwa 20:1
Hes 13:22
Amu 1:9
2Sa 24:7
Oba 19
c Zb 77:12
Zb 143:5
d 1Ko 11:6
e Mwa 18:6
Ebr 11:9
f Mt 19:5
g Mwa 26:8
Efe 5:25
h Mwa 23:2
Mwa 23:19

SURA 25
i Ro 7:2
j Mwa 37:28
Kut 2:15
Hes 22:4
Hes 31:2
Amu 6:2
k 1Nya 1:32
Ayu 2:11
l 1Fa 10:1
m Yer 25:23
Eze 27:20
n Isa 60:6
o 1Nya 1:33

Wote hao walikuwa wana wa
Ketura.
5 Baadaye Abrahamu ali-
mpa Isaka kila kitu alichoku-
wa nacho,[a] **6** lakini wana wa
masuria ambao Abrahamu ali-
kuwa nao Abrahamu aliwapa
zawadi.[b] Kisha alipokuwa bado
hai, akawaagiza waende kuto-
ka kwa Isaka mwana wake,[c]
upande wa mashariki, kwenye
nchi ya Mashariki.[d] **7** Na hizi
ndizo siku za miaka ya maisha
ya Abrahamu alizoishi, miaka
175. **8** Kisha Abrahamu aka-
kata pumzi, akafa katika umri
mwema wa uzee, akiwa mzee
na mwenye kutosheka, naye
akakusanywa kwa watu wake.[e]
9 Basi Isaka na Ishmaeli wa-
nawe wakamzika katika pa-
ngo la Makpela katika sha-
mba la Efroni mwana wa Zo-
hari Mhiti lililoko mbele ya Ma-
mre,[f] **10** lile shamba ambalo
Abrahamu alikuwa amenunua
kutoka kwa wana wa Hethi.
Hapo Abrahamu akazikwa, na
pia Sara mke wake.[g] **11** Ika-
tokea kwamba baada ya kifo
cha Abrahamu, Mungu aliende-
lea kumbariki Isaka mwana
wake,[h] naye Isaka alikuwa aki-
kaa karibu na Beer-lahai-roi.[i]
12 Na hii ndiyo historia ya
Ishmaeli[j] mwana wa Abrahamu
ambaye Hagari Mmisri mjakazi
wa Sara alimzalia Abrahamu.[k]
13 Basi haya ndiyo majina
ya wana wa Ishmaeli, kufuatana
na majina yao, kulingana
na asili za familia zao: Mzali-
wa wa kwanza wa Ishmaeli ali-
kuwa Nebayothi[l] na Kedari[m] na
Adbeeli na Mibsamu[n] **14** na
Mishma na Duma na Masa,
15 Hadadi[o] na Tema,[p] Yeturi,
Nafishi na Kedema.[q] **16** Hao
ndio wana wa Ishmaeli, na
hayo ndiyo majina yao kufua-
tana na nyua zao na kufuata-
na na kambi zao zilizozungu-
shiwa kuta:[a] wakuu kumi na
wawili kulingana na ukoo wao.[b]
17 Na hii ndiyo miaka ya mai-
sha ya Ishmaeli, miaka 137. Ki-
sha akakata pumzi, akafa. Aka-
kusanywa kwa watu wake.[c]
18 Nao wakaanza kukaa kati-
ka mahema tokea Havila[d] kari-
bu na Shuri,[e] ambayo iko mbele
ya Misri, mpaka Ashuru. Mbe-
le ya ndugu zake wote alikaa.[f]
19 Na hii ndiyo historia ya
Isaka mwana wa Abrahamu.[g]
Abrahamu akamzaa Isaka.
20 Na Isaka alikuwa na umri
wa miaka 40 alipomchukua Re-
beka binti ya Bethueli,[h] Msi-
ria,[i] wa Padan-aramu, dada ya
Labani Msiria, awe mke wake.
21 Naye Isaka akaendelea ku-
msihi Yehova hasa kwa aji-
li ya mke wake,[j] kwa sababu
alikuwa tasa;[k] kwa hiyo Yeho-
va akakubali kusihiwa kwa aji-
li yake,[l] na Rebeka mke wake
akapata mimba. **22** Na wale
wana ndani yake wakaanza ku-
pambana,[m] hivi kwamba akase-
ma: "Ikiwa hivi ndivyo ilivyo,
hasa kwa nini niko hai?" Basi
akaenda kumuuliza Yehova.[n]
23 Naye Yehova akamwambia:
"Mataifa mawili yamo tumboni
mwako,[o] na vikundi viwili vya
mataifa vitatenganishwa kuto-
ka tumboni mwako;[p] na kiku-
ndi kimoja cha taifa kitakuwa
chenye nguvu kuliko kile ki-
ngine,[q] na mkubwa atamtumi-
kia mdogo."[r]
24 Mwishowe siku zake za
kuzaa zikatimia, na, tazama!
mapacha walikuwa tumboni
mwake.[s] **25** Kisha yule wa
kwanza akatoka mwekundu

SURA 25

a Mwa 24:36
Met 13:22
Ebr 1:2
b 2Nya 21:3
c Mwa 21:14
Yoh 8:35
Ga 4:30
d Amu 6:3
e Mwa 35:29
Met 9:11
f Mwa 23:9
Mwa 49:30
g Mwa 23:19
h Mwa 17:19
Mwa 26:13
i Mwa 16:14
j Mwa 16:10
k Ga 4:24
l Mwa 36:3
Isa 60:7
m Zb 120:5
Yer 49:28
Eze 27:21
n 1Nya 1:29
o 1Nya 1:30
p Ayu 2:11
Ayu 6:19
q 1Nya 1:31

Safu ya 2

a 1Nya 6:54
Ne 8:16
b Mwa 17:20
Zb 117:1
c Mwa 25:8
d Mwa 2:11
1Sa 15:7
e Mwa 16:7
f Mwa 16:12
g Mwa 22:2
Mt 1:2
h Mwa 22:23
i Kum 26:5
j Kum 4:29
k 1Sa 1:5
l 2Sa 21:14
2Nya 33:13
Lu 1:13
m Ro 9:10
n 1Sa 1:10
o Zb 139:15
Mhu 11:5
p Mwa 36:31
Hes 20:14
q Mwa 27:29
Kum 2:4
r 2Sa 8:14
Mal 1:2
Ro 9:12
s Mwa 38:27

kila mahali kama vazi rasmi la
manyoya;[a] kwa hiyo wakamwi-
ta jina lake Esau.[b] **26** Na ba-
adaye ndugu yake akatoka na
mkono wake ulikuwa unashiki-
lia kisigino cha Esau;[c] kwa hiyo
akaitwa jina lake Yakobo.[d] Na
Isaka alikuwa na umri wa mia-
ka 60 wakati Rebeka alipowa-
zaa.

27 Na wale wavulana waka-
wa wakubwa, naye Esau aka-
wa mwanamume anayejua ji-
nsi ya kuwinda,[e] mwanamume
wa mbugani, bali Yakobo aka-
wa mwanamume asiye na lawa-
ma,[f] akikaa katika mahema.[g]
28 Na Isaka alimpenda Esau,
kwa sababu ilimaanisha nyama
ya mawindo kinywani mwake,
lakini Rebeka alimpenda Yako-
bo.[h] **29** Wakati mmoja Yako-
bo alikuwa anatokosa mchu-
zi, Esau alipofika kutoka mbu-
gani naye alikuwa amechoka.
30 Kwa hiyo Esau akamwa-
mbia Yakobo: "Haraka, tafa-
dhali, nipe nimeze chekundu
—chekundu hicho, kwa maa-
na nimechoka!" Hiyo ndiyo sa-
babu jina lake lilikuwa Edomu.[i]
31 Yakobo akajibu akasema:
"Niuzie, kwanza kabisa, haki
yako ya mzaliwa wa kwanza!"[j]
32 Naye Esau akaendelea ku-
sema: "Tazama mimi ninaka-
ribia kufa, nayo haki ya kuza-
liwa ina faida gani kwangu?"
33 Naye Yakobo akaongeza
hivi: "Niapie kwanza kabisa!"[k]
Naye akamwapia, akamuuzia
Yakobo haki yake ya mzaliwa
wa kwanza.[l] **34** Naye Yakobo
akampa Esau mkate na mchu-
zi wa dengu, naye akala na ku-
nywa.[m] Kisha akaondoka aka-
enda zake. Kwa hiyo Esau ali-
dharau haki ya kuzaliwa.[n]

SURA 25
a Mwa 27:11
2Fa 1:8
Zek 13:4
b Mwa 27:32
Mwa 36:9
Mal 1:3
c Ho 12:3
d Mwa 27:36
Mdo 7:14
e Mwa 27:3
f Zb 37:37
g Ebr 11:9
h Mwa 27:6
Mwa 27:46
i Mwa 36:1
Kum 2:4
Mal 1:4
j Mwa 43:33
Kum 21:17
1Nya 5:1
k Mwa 14:22
Ebr 6:16
l Ebr 12:16
m 1Ko 15:32
n Ayu 21:15
Ayu 34:9

Safu ya 2

SURA 26
a Mwa 12:10
b Mwa 26:26
c Kut 6:3
Hes 12:6
1Yo 4:12
d Kut 32:13
e Mwa 20:1
Ebr 11:9
f Mwa 12:7
Mwa 15:18
Ro 15:8
Ga 4:28
g Mwa 22:16
Zb 105:9
Mik 7:20
Ebr 6:13
h Mwa 15:5
Kum 34:4
Ebr 11:12
i Mwa 12:3
Mwa 22:18
Mdo 3:25
Ga 3:8
j Mwa 17:23
Ebr 11:8
Yak 2:21
k Mwa 26:17
l Mwa 12:13
m Mwa 24:16
n Mwa 24:67
Met 5:18
Mhu 9:9

26 Basi kukatokea njaa ka-
tika nchi hiyo, mbali na
ile njaa ya kwanza iliyotokea
siku za Abrahamu,[a] kwa hiyo
Isaka akaenda kwa Abimele-
ki, mfalme wa Wafilisti, huko
Gerari.[b] **2** Ndipo Yehova aka-
mtokea na kusema:[c] "Usishu-
ke kwenda Misri. Kaa kati-
ka nchi ambayo nitakuonye-
sha.[d] **3** Kaa ukiwa mgeni ka-
tika nchi hii,[e] nami nitaendelea
kuwa pamoja nawe na kuku-
bariki, kwa sababu nitakupa
wewe na uzao wako nchi zote
hizi,[f] nami nitaitimiza ahadi
yenye kiapo ambayo nili-
mwapia Abrahamu baba yako,[g]
4 'Nami nitauzidisha uzao
wako kama nyota za mbinguni.
Nami nitaupa uzao wako nchi
zote hizi;[h] na kupitia uzao wako
mataifa yote ya dunia yatajiba-
riki,'[i] **5** kwa sababu ya uhaki-
ka wa kwamba Abrahamu ali-
sikiliza sauti yangu na kuen-
delea kushika wajibu wake
kwangu, amri zangu, mashar-
ti yangu, na sheria zangu."[j]
6 Kwa hiyo Isaka akaendelea
kukaa huko Gerari.[k]

7 Basi, wanaume wa mahali
hapo wakawa wakiuliza juu ya
mke wake, naye akawa akise-
ma: "Yeye ni dada yangu."[l]
Kwa maana aliogopa kusema
"Ni mke wangu" kwa kuogo-
pa kwamba, kama alivyosema,
"wanaume wa mahali hapa wa-
taniua kwa sababu ya Rebe-
ka," kwa sababu alikuwa mwe-
nye sura ya kuvutia.[m] **8** Basi,
siku zake huko zilipoongeze-
ka, Abimeleki, mfalme wa Wafi-
listi, alikuwa akiangalia nje di-
rishani na kutazama mazingi-
ra, na tazama, Isaka alikuwa
anachezacheza pamoja na Re-
beka mke wake.[n] **9** Mara

moja Abimeleki akamwita Isaka na kusema: “Kumbe, si mwingine bali ni mke wako! Kwa hiyo kwa nini ulisema, ‘Yeye ni dada yangu’?” Isaka akamjibu, akamwambia: “Nilisema hivyo kwa kuogopa nisije nikafa kwa sababu yake.”[a] **10** Lakini Abimeleki akaendelea kusema: “Ni nini hili umetutendea sisi?[b] Ilibaki kitambo kidogo tu na mmoja kati ya watu angelala na mke wako, nawe ungeleta hatia juu yetu!”[c] **11** Ndipo Abimeleki akawaamuru watu wote, akisema: “Yeyote atakayemgusa mwanamume huyu na mke wake bila shaka atauawa!”

12 Baadaye Isaka akaanza kupanda mbegu katika nchi hiyo,[d] na mwaka huo alikuwa akipata kufikia vipimo mia moja kwa kimoja,[e] kwa kuwa Yehova alikuwa anambariki.[f] **13** Basi huyo mwanamume akawa mkuu na kuendelea kusonga zaidi na zaidi na kuwa mkuu mpaka akawa mkuu sana.[g] **14** Naye akaja kuwa na makundi ya kondoo na mifugo ya ng’ombe na kundi kubwa la watumishi,[h] hivi kwamba Wafilisti wakaanza kumwonea wivu.[i]

15 Navyo visima vyote ambavyo watumishi wa baba yake walikuwa wamechimba siku za Abrahamu baba yake,[j] Wafilisti wakawa wakivifunika na kuvijaza kwa udongo mkavu.[k] **16** Mwishowe Abimeleki akamwambia Isaka: “Ondoka katika ujirani wetu, kwa sababu umepata nguvu mno kuliko sisi.”[l] **17** Kwa hiyo Isaka akahama kutoka huko na kupiga kambi katika bonde la mto la Gerari[m] na kuanza kukaa huko. **18** Naye Isaka akaanza tena kuchimba visima vya maji ambavyo walikuwa wamechimba siku za Abrahamu baba yake lakini ambavyo Wafilisti walikuwa wameviziba baada ya kifo cha Abrahamu;[a] naye akaviita tena kwa majina yale ambayo baba yake alikuwa ameviita.[b]

19 Watumishi wa Isaka wakaendelea kuchimba katika bonde la mto na basi wakapata huko kisima cha maji safi. **20** Nao wachungaji wa Gerari wakaanza kugombana na wachungaji wa Isaka,[c] wakisema: “Maji haya ni yetu!” Basi akakiita hicho kisima Eseki, kwa sababu walikuwa wameshindana naye. **21** Nao wakachimba kisima kingine, nao wakaanza kukigombania pia. Basi akakiita Sitna. **22** Baadaye akahama kutoka huko na kuchimba kisima kingine,[d] lakini hawakukigombania. Basi akakiita Rehobothi na kusema: “Ni kwa sababu sasa Yehova ametupa sisi nafasi ya kutosha[e] naye ametufanya tuongezeke duniani.”[f]

23 Kisha akapanda kutoka huko mpaka Beer-sheba.[g] **24** Naye Yehova akamtokea usiku huo na kusema: “Mimi ni Mungu wa Abrahamu baba yako.[h] Usiogope,[i] kwa sababu mimi nipo pamoja nawe, nami nitakubariki wewe na kuuzidisha uzao wako kwa sababu ya Abrahamu mtumishi wangu.”[j] **25** Basi akajenga madhabahu huko, akaliitia jina la Yehova[k] na kupiga hema lake huko,[l] na watumishi wa Isaka wakachimba kisima huko.

26 Baadaye Abimeleki akamjia kutoka Gerari pamoja na

SURA 26

a Mwa 20:11
b Mwa 12:18
c Mwa 20:9
Mwa 39:9
Met 6:29
Ebr 13:4
d Mwa 8:22
Isa 55:10
2Ko 9:10
e 1Ko 3:6
f Mwa 24:1
Ayu 42:12
Zb 3:8
Zb 67:6
Met 10:22
Ebr 6:7
g Mwa 24:35
h Mwa 12:16
Ayu 1:3
i Mwa 37:11
1Sa 18:9
Met 27:4
Ro 1:29
Tit 3:3
j Mwa 21:30
k Met 25:26
l Kut 1:9
Zb 105:24
m Mwa 10:19
Mwa 20:1

Safu ya 2

a Mwa 21:25
b Mwa 21:31
c Mwa 13:7
d Mwa 13:9
Met 17:14
Ro 12:18
e Law 26:9
Zb 18:19
Zb 118:5
f Mwa 17:6
Mwa 28:3
Eze 36:11
g Mwa 21:31
h Mwa 17:1
Mwa 28:13
Kut 3:6
Mt 22:32
Mdo 7:32
i Mwa 15:1
Kum 31:8
Zb 27:1
Ebr 13:6
j Mwa 17:19
Zb 105:9
Ga 3:29
k Mwa 12:8
Ro 10:13
l Mwa 4:20
Ebr 11:9

Ahuzathi rafiki yake wa karibu na Fikoli mkuu wa jeshi lake.[a] **27** Basi Isaka akawaambia: "Kwa nini ninyi mmekuja kwangu, hali ninyi wenyewe mlinichukia na kwa sababu hiyo mkaniagiza nitoke katika ujirani wenu?"[b] **28** Wakajibu, wakasema: "Bila shaka sisi tumeona kwamba Yehova amekuwa pamoja nawe.[c] Hivyo tukasema, 'Tafadhali, kiapo cha wajibu na kiwepo kati yetu,[d] kati yetu na wewe, nasi na tufanye agano pamoja nawe,[e] **29** kwamba wewe hutafanya lolote baya kutuelekea kama vile ambavyo sisi hatukukugusa wewe na kama vile ambavyo sisi tumetenda wema tu kukuelekea kwa kuwa tulikuagiza uende kwa amani.[f] Wewe sasa ni mbarikiwa wa Yehova.'"[g] **30** Kisha akawafanyia karamu nao wakala na kunywa.[h] **31** Asubuhi iliyofuata waliamka mapema nao wakatoleana ahadi zenye kiapo.[i] Baada ya hayo Isaka akawaacha waende zao nao wakaondoka kwake kwa amani.[j]

32 Ndipo siku hiyo ikatukia kwamba watumishi wa Isaka walikuja na kumpa habari kuhusu kisima ambacho walikuwa wamechimba,[k] na kumwambia: "Tumepata maji!" **33** Hivyo akakiita Shiba. Hiyo ndiyo sababu jina la jiji hilo ni Beer-sheba[l] mpaka leo hii.

34 Na Esau akafikia umri wa miaka 40. Kisha akamchukua Yudithi binti ya Beeri, Mhiti, kuwa mke na pia Basemathi binti ya Eloni, Mhiti.[m] **35** Nao walikuwa chanzo cha uchungu wa roho kwa Isaka na Rebeka.[n]

SURA 26
a Mwa 21:32
b Amu 11:7
c Mwa 21:22
Mwa 39:5
Yos 3:7
Zek 8:23
1Ko 14:25
d Mwa 21:31
e Mwa 21:27
Mwa 31:44
f Met 16:7
g Mwa 12:2
Mwa 22:17
Zb 115:15
Isa 61:9
Mt 25:34
h Mwa 19:3
2Fa 6:23
i Mwa 14:22
Mwa 21:23
1Sa 20:17
j Ro 12:18
Ebr 12:14
1Pe 3:11
k Mwa 26:18
l Amu 20:1
m Mwa 36:2
Kum 7:3
n Mwa 27:46
Mwa 28:8

Safu ya 2

SURA 27
a Mwa 48:10
Mhu 12:3
b Mwa 25:28
c Isa 46:4
d Mwa 48:21
Met 27:1
Mhu 9:12
Yak 4:14
e Mwa 25:27
f Mwa 48:9
Mwa 49:28
Ebr 11:20
g Mwa 27:30
h Mwa 25:28
i Mwa 27:31
Mwa 49:1
Kum 33:1
j Mwa 27:13
Mwa 27:43
Met 1:8
Efe 6:1

27 Na ikawa kwamba Isaka alipokuwa mzee na macho yake yalikuwa yameingia giza mno asiweze kuona,[a] akamwita Esau mwana wake mkubwa na kumwambia:[b] "Mwanangu!" naye akamjibu: "Mimi hapa!" **2** Naye akaendelea kusema: "Tazama, mimi sasa nimekuwa mzee.[c] Sijui siku ya kifo changu.[d] **3** Kwa hiyo wakati huu chukua, tafadhali, vifaa vyako, podo lako na upinde wako, uende nje mbugani uniwindie mawindo fulani.[e] **4** Kisha nifanyie chakula kitamu, kile ninachokipenda sana, halafu uniletee na, ah, acha nile, ili kwamba nafsi yangu ipate kukubariki wewe kabla ya kufa kwangu."[f]

5 Hata hivyo, Rebeka alikuwa akisikiliza Isaka alipokuwa akisema na Esau mwana wake. Esau akaenda nje mbugani awinde mawindo ayalete.[g] **6** Naye Rebeka akamwambia Yakobo mwana wake:[h] "Tazama, mimi sasa hivi nimemsikia baba yako akimwambia Esau ndugu yako, akisema, **7** 'Niletee mawindo fulani unifanyie chakula kitamu na, ah, acha nile, ili nipate kukubariki wewe mbele za Yehova kabla ya kifo changu.'[i] **8** Na sasa, mwanangu, sikiliza sauti yangu katika lile ninalokuamuru.[j] **9** Tafadhali nenda kundini uniletee kutoka humo wanambuzi wawili wazuri, ili nipate kuwatayarisha wawe chakula kitamu kwa ajili ya baba yako, chakula kile anachokipenda sana. **10** Kisha ukilete kwa baba yako naye apate kula, ili akubariki wewe kabla ya kifo chake."

11 Naye Yakobo akamwambia Rebeka mama yake: "Lakini Esau ndugu yangu ni mwanamume mwenye nywele nyingi mwilini nami ni mwanamume mwenye ngozi laini.[a] **12** Namna gani baba yangu akinipapasa?[b] Ndipo hakika nitakuwa machoni pake kama mtu anayefanya mzaha,[c] nami hakika nitajiletea laana wala si baraka."[d] **13** Ndipo mama yake akajibu, akamwambia: "Laana uliyokusudiwa wewe na iwe juu yangu, mwanangu.[e] Ila tu sikiliza sauti yangu na uende, uniletee hao."[f] **14** Basi akaenda, akawapata, akawaleta kwa mama yake, naye mama yake akatayarisha chakula kitamu namna ambavyo baba yake alipenda sana. **15** Kisha Rebeka akachukua mavazi ya Esau mwana wake mkubwa,[g] yale yenye kupendeza zaidi ambayo alikuwa nayo nyumbani,[h] akamvika Yakobo mwana wake mdogo.[i] **16** Akaweka ngozi za wana-mbuzi hao juu ya mikono yake na juu ya sehemu isiyo na nywele ya shingo yake.[j] **17** Kisha akatia kile chakula kitamu na mkate aliokuwa ametayarisha mkononi mwa Yakobo mwana wake.[k]

18 Kwa hiyo akaingia ndani kwa baba yake na kusema: "Baba yangu!" naye akasema: "Mimi hapa! Wewe ni nani, mwanangu?" **19** Naye Yakobo akaendelea kumwambia baba yake: "Mimi ni Esau mzaliwa wako wa kwanza.[l] Nimefanya kama vile ulivyoniambia. Inuka, tafadhali. Keti ule sehemu ya mawindo yangu, ndipo nafsi yako ipate kunibariki."[m] **20** Basi Isaka akamwambia mwana wake: "Imekuwaje kwamba umeyapata upesi sana, mwanangu?" Naye akasema: "Kwa sababu Yehova Mungu wako alifanya mawindo yakutane nami." **21** Ndipo Isaka akamwambia Yakobo: "Tafadhali, njoo karibu ili nikupapase, mwanangu, nijue kama kwa kweli wewe ni mwanangu Esau au sivyo."[a] **22** Kwa hiyo Yakobo akamkaribia Isaka baba yake, naye akaanza kumpapasa, ndipo akasema: "Sauti ni sauti ya Yakobo, lakini mikono ni mikono ya Esau."[b] **23** Naye hakumtambua, kwa sababu mikono yake ilikuwa na nywele nyingi kama mikono ya Esau ndugu yake. Kwa hiyo akambariki.[c]

24 Baada ya hayo akasema: "Wewe kwa kweli ni mwanangu Esau?" naye akasema: "Ni mimi."[d] **25** Kisha akasema: "Leta karibu nami, nipate kula sehemu ya mawindo ya mwanangu, ndipo nafsi yangu ikubariki."[e] Basi akaleta karibu naye, naye akaanza kula, akaletewa divai naye akaanza kunywa. **26** Kisha Isaka baba yake akamwambia: "Njoo karibu, tafadhali, unibusu, mwanangu."[f] **27** Kwa hiyo akaja karibu akambusu, naye akanusa harufu ya mavazi yake.[g] Naye akaanza kumbariki akisema:

"Tazama, harufu ya mwanangu ni kama harufu ya shamba ambalo Yehova amebariki. **28** Mungu wa kweli na akupe umande wa mbinguni[h] na udongo wenye rutuba wa dunia[i] na wingi wa nafaka na divai mpya.[j] **29** Vikundi vya watu na vikutumikie na vikundi vya mataifa vikuinamie.[k] Uwe bwana wa ndugu zako, na wana wa mama yako na wakuinamie.[l]

SURA 27

a Mwa 25:25
Mwa 27:23
b Mwa 27:21
c Yos 9:6
d Kum 11:26
Kum 23:5
Kum 30:1
e Mwa 43:9
f Mwa 27:8
Met 6:20
g Mwa 25:23
h 1Sa 28:8
i Mwa 25:26
j Mwa 25:25
Mwa 27:11
k Mwa 27:9
l Mwa 25:33
Ro 9:12
m Mwa 27:4
Ebr 11:20

Safu ya 2

a Mwa 27:11
b Mwa 27:16
c Kum 21:17
Ro 9:11
Ebr 11:20
d Mwa 25:33
e Kum 33:28
Met 10:6
f Mwa 48:10
g Mwa 25:27
Mwa 27:15
Wim 4:11
h Kum 11:11
Isa 45:8
Ho 14:5
i Mwa 45:18
Hes 13:27
j Mwa 27:37
Kum 7:13
2Fa 18:32
Zb 104:15
k 2Sa 8:1
Da 2:44
l Mwa 25:23
Mwa 49:8

Na alaaniwe kila mmoja wa
wale wanaokulaani, na abariki-
we kila mmoja wa wale wanao-
kubariki."[a]
30 Basi ikawa mara tu Isaka
alipokuwa amemaliza kumba-
riki Yakobo, ndiyo, kwa kwe-
li ikawa hapo tu Yakobo ali-
pokuwa ametoka mbele ya uso
wa Isaka baba yake, Esau ndu-
gu yake akarudi kutoka katika
uwindaji wake.[b] **31** Naye pia
akaanza kutayarisha chaku-
la kitamu. Kisha akakileta kwa
baba yake na kumwambia baba
yake: "Baba yangu na ainuke
ale sehemu ya mawindo ya
mwana wake, ndipo nafsi yako
inibariki."[c] **32** Isaka, baba
yake, akamjibu, akamwambia:
"Wewe ni nani?" naye akasema:
"Mimi ni mwana wako, mza-
liwa wako wa kwanza, Esau."[d]
33 Naye Isaka akaanza kutete-
meka kwa tetemeko kubwa
sana, na kusema: "Ni nani, basi,
aliyewinda mawindo akaja ku-
niletea, hivi kwamba nikala
kila kitu kabla ya wewe kuingia
nami nikambariki? Ndiyo, yeye
pia atabarikiwa!"[e]
34 Aliposikia maneno ya
baba yake, Esau akaanza ku-
paaza kilio kwa sauti ku-
bwa na yenye uchungu na ku-
mwambia baba yake:[f] "Nibariki
mimi, hata mimi pia, baba ya-
ngu!"[g] **35** Lakini yeye akaen-
delea kusema: "Ndugu yako
alikuja kwa udanganyifu ili
aweze kupata baraka uliyoku-
sudiwa."[h] **36** Akajibu, akase-
ma: "Je, hiyo siyo sababu jina
lake ni Yakobo, hivi kwamba
anyakue mahali pangu mara
mbili hizi?[i] Haki yangu ya ku-
zaliwa tayari amechukua,[j] na
tazama wakati huu amechu-
kua baraka yangu!"[k] Kisha aka-

SURA 27

a Mwa 12:3
Mwa 28:3
Mwa 31:42
Hes 24:9
Eze 25:12
b Mwa 27:3
c Ebr 7:7
d Mwa 25:25
Mwa 25:31
Ebr 12:16
e Ro 9:13
f Lu 13:28
g Ebr 12:17
h Kum 21:17
Mal 1:2
Ga 3:9
i Mwa 25:26
Mwa 32:28
Ho 12:3
j Mwa 25:34
Mt 5:33
Ebr 6:16
k Mwa 27:28

Safu ya 2

a Mwa 25:23
Mwa 27:29
Ro 9:12
b Mwa 49:8
c Kum 33:28
Yoe 2:19
d Ebr 12:17
e Isa 65:14
f Yos 24:4
Ebr 11:20
g Mwa 32:6
Hes 20:18
h Mwa 25:23
2Sa 8:14
i 2Fa 8:20
2Nya 28:17
j Mwa 4:5
Mwa 37:11
Amo 1:11
1Yo 2:11
k Zb 140:2
Mk 7:21
l Mwa 35:29
m Mwa 4:8
1Yo 3:15
n Mwa 37:18
Zb 64:6
Met 6:17

ongeza: "Je, hukuniachia ba-
raka yoyote?" **37** Lakini Isa-
ka akamjibu Esau na kuendelea
kusema: "Tazama nimemwe-
ka awe bwana juu yako,[a] na ndu-
gu zake wote nimempa kuwa
watumishi,[b] na nafaka na di-
vai mpya nimetoa ili kumte-
gemeza,[c] basi liko wapi lolote
ninaloweza kukufanyia, mwa-
nangu?"
38 Kisha Esau akamwambia
baba yake: "Je, huna hata bara-
ka moja tu, baba yangu? Nibari-
ki mimi, hata mimi pia, baba
yangu!"[d] Kisha Esau akapaaza
sauti yake na kuanza ku-
lia machozi.[e] **39** Basi Isaka
baba yake akajibu, akamwa-
mbia:
"Tazama, makao yako ya-
takuwa mbali na udongo we-
nye rutuba wa dunia, na mba-
li na umande wa mbingu juu.[f]
40 Nawe utaishi kwa upanga
wako,[g] na kumtumikia ndu-
gu yako.[h] Lakini itatokea
kwamba, utakapokosa utuli-
vu, wewe hakika utavunja nira
yake kutoka shingoni pako."[i]
41 Hata hivyo, Esau akawe-
ka uadui kumwelekea Yakobo
kwa sababu ya baraka amba-
yo baba yake alikuwa ame-
mbarikia,[j] na Esau akaende-
lea kusema moyoni mwake:[k]
"Siku za kipindi cha kuombole-
za baba yangu zinakaribia.[l]
Baada ya hizo nitamuua Ya-
kobo ndugu yangu."[m] **42** Re-
beka alipojulishwa maneno ya
Esau mwana wake mkubwa,
mara moja akapeleka haba-
ri na kumwita Yakobo mwa-
na wake mdogo, akamwambia:
"Tazama! Esau ndugu yako
anajifariji kukuhusu—kukuua
wewe.[n] **43** Sasa, basi, mwa-
nangu, sikiliza sauti yangu,

ondoka,[a] ukimbilie kwa Labani ndugu yangu huko Harani.[b]
44 Nawe ukae naye kwa siku kadhaa mpaka ghadhabu ya ndugu yako itulie,[c] **45** mpaka hasira ya ndugu yako igeukie mbali nawe, naye awe amesahau yale uliyomtendea.[d] Nami kwa hakika nitapeleka habari nikuchukue kutoka huko. Kwa nini nifiwe pia na ninyi wawili siku moja?"

46 Baada ya hayo Rebeka akawa akimwambia Isaka: "Nimekuja kuyachukia sana haya maisha yangu kwa sababu ya binti za Hethi.[e] Yakobo akichukua mke kutoka kwa binti za Hethi kama hawa kutoka kwa binti za hii nchi, basi maisha yana faida gani kwangu?"[f]

28 Basi Isaka akamwita Yakobo akambariki na kumwamuru akisema: "Usichukue mke kutoka kwa binti za Kanaani.[g] **2** Ondoka, uende mpaka Padan-aramu kwa nyumba ya Bethueli baba ya mama yako na kutoka huko ujichukulie mke kati ya binti za Labani ndugu ya mama yako.[h]
3 Na Mungu Mweza-Yote atakubariki na kukufanya uzae na kukuzidisha, nawe utakuwa kutaniko la vikundi vya watu.[i] **4** Naye atakupa baraka ya Abrahamu,[j] wewe na uzao wako pamoja nawe,[k] ili upate kumiliki nchi ya makao yako ya kigeni,[l] ambayo Mungu amempa Abrahamu."[m]

5 Kwa hiyo Isaka akamwacha Yakobo aende, naye akafunga safari kwenda Padan-aramu, kwa Labani mwana wa Bethueli Msiria,[n] ndugu ya Rebeka,[o] mama ya Yakobo na Esau.[p]

6 Esau alipoona kwamba Isaka alikuwa amembariki Yakobo akamwacha aende Padan-aramu ajichukulie kutoka huko mke, na kwamba alipombariki aliweka juu yake amri, akisema: "Usichukue mke kati ya binti za Kanaani";[a] **7** na kwamba Yakobo alikuwa akimtii baba yake na mama yake naye alikuwa ameondoka kwenda Padan-aramu;[b] **8** ndipo Esau akaona kwamba binti za Kanaani walikuwa wasiopendeza machoni pa Isaka baba yake.[c] **9** Kwa hiyo Esau akaenda kwa Ishmaeli akamchukua Mahalathi binti ya Ishmaeli mwana wa Abrahamu, dada ya Nebayothi, kuwa mke wake, kuongezea wake zake wengine.[d]

10 Na Yakobo akazidi kwenda zake kutoka Beer-sheba, akaendelea mpaka Harani.[e]
11 Mwishowe akafika mahali fulani, akaanza kukaa hapo usiku huo kwa sababu jua lilikuwa limetua. Kwa hiyo akachukua moja la mawe ya mahali hapo akaliweka kuwa kitu cha kutegemeza kichwa chake, akalala mahali hapo.[f]
12 Naye akaanza kuota ndoto,[g] na, tazama! kulikuwa na ngazi iliyosimamishwa juu ya dunia na kilele chake kilikuwa kimefika mbinguni; na, tazama! malaika za Mungu walikuwa wakipanda na kushuka juu yake.[h] **13** Na, tazama! Yehova alikuwa amesimama juu yake, naye akaanza kusema:[i]

"Mimi ni Yehova Mungu wa Abrahamu baba yako na Mungu wa Isaka.[j] Nchi ambayo unalala juu yake, nitakupa wewe na uzao wako.[k] **14** Na uzao wako utakuwa kama chembe za mavumbi ya dunia,[l] nawe hakika utaenea koteko-

SURA 27
a Mt 1:8; Kol 3:20
b Mwa 28:5
c Zb 37:8
d Kut 4:19; Mt 5:22
e Mwa 26:35; Mwa 28:8
f Mwa 24:3

SURA 28
g Mwa 24:37; Kut 34:15; 1Fa 11:1; 1Ko 7:39; 2Ko 6:14
h Mwa 29:16
i Mwa 17:5; Mwa 46:15; 1Nya 2:1; Ro 4:17
j Mwa 12:2
k Mwa 15:5; Ro 9:7; Ga 3:29
l Mwa 12:7; Mwa 15:13; Mwa 17:8
m Ebr 11:9
n Mwa 25:20
o Mwa 24:29
p Mwa 25:28

Safu ya 2
a Mwa 28:1; 2Ko 6:14
b Mwa 27:43; Kut 20:12; Law 19:3
c Mwa 24:3; Mwa 27:46
d Mwa 36:2
e Mwa 11:31; Mwa 27:43
f Mwa 28:19
g Hes 12:6; Ayu 33:15
h Mt 28:2; Yoh 1:51; Ebr 1:14
i Da 7:9
j Mwa 26:24; Mk 12:26; Mdo 7:32
k Mwa 12:7; Mwa 28:4; Zb 105:11; Mdo 7:5
l Mwa 13:16; 1Fa 4:20

te upande wa magharibi na wa
mashariki na wa kaskazini na
wa kusini,[a] na kupitia kwako
na kupitia kwa uzao wako fa-
milia zote za nchi hakika zita-
jibariki.[b] **15** Na tazama, mimi
nipo pamoja nawe, nami nita-
kutunza katika njia yote una-
yoenda, nami nitakurudisha
kwenye nchi hii,[c] kwa sababu
sitakuacha mpaka niwe kwa
kweli nimefanya hayo ambayo
nimekuambia."[d]

16 Kisha Yakobo akaamka
katika usingizi wake, akase-
ma: "Kwa kweli Yehova yupo
mahali hapa na mimi mwe-
nyewe sikujua hilo." **17** Naye
akaogopa, akaongeza kusema:[e]
"Jinsi mahali hapa panavyo-
ogopesha![f] Bila shaka maha-
li hapa ni nyumba ya Mungu[g]
napo ndipo lango la mbingu-
ni." **18** Kwa hiyo Yakobo aka-
amka asubuhi na mapema, aka-
chukua jiwe lililokuwa hapo
kama kitu cha kutegemeza ki-
chwa chake, naye akalisimami-
sha kama nguzo na kumimina
mafuta juu yake.[h] **19** Tena,
akaita jina la mahali hapo Be-
theli,[i] lakini ukweli ni kwamba,
hapo zamani jina la jiji hilo lili-
kuwa ni Luzi.[j]

20 Ndipo Yakobo akaweka
nadhiri,[k] akisema: "Mungu aki-
endelea kuwa pamoja nami na
kwa hakika anitunze katika
njia hii ninayoiendea na kuni-
pa mkate wa kula na mavazi
ya kuvaa[l] **21** nami hakika ni-
rudi kwa amani nyumbani kwa
baba yangu, basi Yehova ata-
kuwa amejionyesha kuwa Mu-
ngu wangu.[m] **22** Na jiwe hili
ambalo nimesimamisha kuwa
nguzo litakuwa nyumba ya Mu-
ngu,[n] na katika kila kitu uta-

SURA 28

a Mwa 13:14
b Mwa 18:18
Mwa 22:18
c Mwa 35:6
Mwa 46:4
d Mwa 31:3
Hes 23:19
Yos 23:14
Ebr 6:18
e Kut 3:6
Amu 13:22
Mt 17:6
f Zb 47:2
Zb 66:5
Zb 68:35
g Mwa 35:1
Zb 27:4
h Mwa 31:13
i Amu 4:5
Ho 12:4
j Mwa 35:6
Yos 16:2
Amu 1:23
k Mhu 5:4
l Mt 6:30
m Kut 15:2
Kum 26:17
n Mwa 35:1

Safu ya 2

a Mwa 14:20
Law 27:30
Mal 3:8

SURA 29

b Amu 6:3
1Fa 4:30
Ayu 1:3
c Mwa 30:40
Wim 4:1
d Mwa 24:11
Kut 2:15
Yoh 4:6
e Mwa 27:43
Mdo 7:2
f Mwa 24:29
g Mwa 24:24
Mwa 31:53
h Mwa 43:27
1Sa 17:22
i Mwa 31:4
Mwa 46:19
Ru 4:11
j Kut 2:16
k Zb 23:2
Wim 1:7
l Mwa 30:1
Mwa 35:19

kachonipa bila shaka nitakupa
wewe sehemu ya kumi."[a]

29 Kisha Yakobo akaanza
mwendo, akasafiri kwe-
nda nchi ya Watu wa Masha-
riki.[b] **2** Basi akatazama, na
hapo palikuwa na kisima sha-
mbani na tazama, makundi
matatu ya kondoo yalikuwa ya-
melala chini hapo kando yake,
kwa sababu walikuwa na de-
sturi ya kunywesha maji ma-
kundi[c] katika kisima hicho; na
kulikuwa na jiwe kubwa juu
ya kinywa cha hicho kisima.[d]
3 Makundi yote yalipokuwa
yamekusanywa hapo, waliviri-
ngisha jiwe kutoka kwenye
kinywa cha kisima, nao wa-
kanywesha makundi maji, ki-
sha wakalirudisha jiwe mahali
pake juu ya kinywa cha kisima.

4 Basi Yakobo akawaambia:
"Ndugu zangu, mmetoka
wapi?" nao wakasema: "Sisi
tunatoka Harani."[e] **5** Ndi-
po akawaambia: "Je, mna-
mjua Labani[f] mjukuu wa Na-
hori?"[g] nao wakasema: "Tu-
namjua." **6** Basi akawaambia:
"Je, yeye hajambo?"[h] Nao wa-
kasema: "Hajambo. Na ta-
zama, Raheli[i] binti yake anaku-
ja na kondoo!"[j] **7** Naye akae-
ndelea kusema: "Tazama, bado
ni mchana sana. Sio wakati wa
kukusanya mifugo. Wanywe-
sheni maji kondoo, kisha mwe-
nde mwalishe."[k] **8** Wakajibu,
wakasema: "Haturuhusiwi ku-
fanya hivyo mpaka makundi
yote yawe yamekusanywa nao
kwa kweli wawe wameviringi-
sha jiwe kutoka kwenye ki-
nywa cha kisima. Ndipo tutaka-
ponywesha kondoo maji."

9 Alipokuwa bado anasema
nao, Raheli[l] akaja na kondoo

wa baba yake, kwa maana ali-
kuwa mchungaji.[a] **10** Ikawa
kwamba Yakobo alipomwona
Raheli binti ya Labani ndugu
ya mama yake na kondoo wa
Labani ndugu ya mama yake,
bila kukawia Yakobo akakarib-
ia na kuliviringisha jiwe, aka-
liondoa kwenye kinywa cha hi-
cho kisima na kuwanywesha
maji kondoo wa Labani ndugu
ya mama yake.[b] **11** Kisha Ya-
kobo akambusu[c] Raheli, akapa-
aza sauti yake na kulia macho-
zi.[d] **12** Na Yakobo akaanza
kumwambia Raheli kwamba
yeye ni ndugu[e] ya baba yake
na kwamba yeye ni mwana
wa Rebeka. Na Raheli aka-
kimbia, akaenda kumwambia
baba yake.[f]

13 Sasa ikawa kwamba
mara tu Labani alipoisikia
habari juu ya Yakobo mwa-
na wa dada yake, akaanza ku-
kimbia kwenda kumpokea.[g]
Kisha akamkumbatia na ku-
mbusu, akamleta mpaka ndani
ya nyumba yake.[h] Naye akaa-
nza kumsimulia Labani mambo
hayo yote. **14** Baada ya hayo
Labani akamwambia: "Wewe
kwa kweli ni mfupa wangu na
nyama yangu."[i] Basi akakaa
naye mwezi mzima.

15 Kisha Labani akamwa-
mbia Yakobo: "Je, wewe ni
ndugu yangu,[j] na je, unitu-
mikie bure?[k] Niambie, Msha-
hara wako utakuwa nini?"[l]
16 Basi, Labani alikuwa na bi-
nti wawili. Jina la yule mku-
bwa lilikuwa ni Lea[m] na jina
la yule mdogo Raheli. **17** La-
kini macho ya Lea hayakuwa
yaking'aa, bali Raheli[n] aliku-
wa na umbo zuri na sura nzuri.[o]
18 Naye Yakobo alimpenda Ra-
heli. Kwa hiyo akasema: "Mimi
niko tayari kukutumikia mia-
ka saba kwa ajili ya Raheli bi-
nti yako mdogo."[a] **19** Laba-
ni akajibu akasema: "Ni afa-
dhali nikupe wewe kuliko ni-
mpe mwanamume mwingine.[b]
Endelea kukaa pamoja nami."
20 Naye Yakobo akatumikia
miaka saba kwa ajili ya Raheli,[c]
lakini machoni pake hiyo ika-
wa kama siku chache kwa sa-
babu alimpenda.[d]

21 Kisha Yakobo akamwa-
mbia Labani: "Nipe mke wa-
ngu, kwa sababu siku za-
ngu zimetimia, nawe uniru-
husu nilale naye."[e] **22** Basi
Labani akawakusanya watu
wote wa mahali hapo, akafa-
nya karamu.[f] **23** Lakini ika-
wa kwamba wakati wa jioni
akamchukua Lea binti yake,
akamleta kwa Yakobo ili apa-
te kulala naye. **24** Pia, Labani
akampa Lea binti yake mjaka-
zi wake Zilpa,[g] awe mjakazi
wake. **25** Basi kufika asubuhi
akakuta kumbe ni Lea!
Kwa hiyo akamwambia Laba-
ni: "Ni nini hili umenitendea?
Je, sikukutumikia kwa ajili
ya Raheli? Basi kwa nini ume-
nifanyia ujanja?"[h] **26** Laba-
ni akajibu akasema: "Si de-
sturi kufanya hivi kwetu, ku-
mtoa mwanamke mdogo ka-
bla ya mzaliwa wa kwanza.
27 Sherehekea[i] kikamili juma
la mwanamke huyu. Baada-
ye utapewa pia mwanamke
huyu mwingine kwa utumishi
ambao wewe unaweza kunitu-
mikia kwa miaka saba zaidi."[j]
28 Basi Yakobo akafanya hi-
yo, akasherehekea kikamili
juma la mwanamke huyo, ba-
ada ya hayo akampa Rahe-
li binti yake kuwa mke wake.

SURA 29
a Kut 2:16
b Kut 2:17
c Mwa 33:4
Mwa 45:15
Lu 15:20
Ro 16:16
d Mwa 43:30
Mwa 45:2
e Mwa 13:8
Mwa 14:14
f Mwa 24:28
g Mwa 24:29
h Mdo 20:37
i Amu 9:2
2Sa 5:1
j Mwa 27:43
Mwa 28:5
k Kum 25:4
1Ti 5:18
l Mwa 30:28
Mwa 31:7
m Mwa 30:19
Mwa 46:15
Ru 4:11
n Mwa 30:25
Mwa 35:16
o Mwa 12:11
Mwa 24:16
Est 2:7

Safu ya 2
a Mwa 31:41
Mwa 34:12
b Zb 12:2
c Mwa 30:26
Ho 12:12
d Wim 8:6
e Ru 4:13
Met 5:18
1Ko 7:3
f Amu 14:10
Mt 22:2
Ufu 19:9
g Mwa 16:1
Mwa 30:9
Mwa 46:18
h Mwa 31:7
Mwa 31:42
Law 19:11
Mt 5:37
2Ko 4:2
i Kum 24:5
Zb 19:5
j Mwa 31:41

29 Tena, Labani akampa Raheli binti yake Bilha[a] mjakazi wake, awe mjakazi wake.

30 Kisha akalala na Raheli pia, naye akamwonyesha Raheli upendo zaidi kuliko Lea,[b] naye akamtumikia Labani kwa miaka saba zaidi.[c] **31** Yehova alipoona kwamba Lea alichukiwa, ndipo akafungua tumbo lake la uzazi,[d] lakini Raheli alikuwa tasa.[e] **32** Basi Lea akapata mimba, akazaa mwana na kisha akamwita jina lake Rubeni,[f] kwa maana alisema: "Ni kwa sababu Yehova ametazama taabu yangu,[g] kwa kuwa sasa mume wangu ataanza kunipenda." **33** Naye akapata mimba tena, akazaa mwana kisha akasema: "Ni kwa sababu Yehova amesikiliza,[h] kwa kuwa nilichukiwa na kwa hiyo akanipa huyu pia." Ndipo akamwita jina lake Simeoni.[i] **34** Naye akapata mimba tena, akazaa mwana kisha akasema: "Sasa wakati huu mume wangu atajiunga nami, kwa sababu nimemzalia wana watatu." Kwa hiyo akaitwa jina lake Lawi.[j] **35** Naye akapata mimba tena, akazaa mwana kisha akasema: "Mara hii nitamsifu Yehova." Kwa hiyo akamwita jina lake Yuda.[k] Kisha akaacha kuzaa.

30 Raheli alipoona kwamba alikuwa hajamzalia Yakobo mwana yeyote, Raheli akamwonea wivu dada yake naye akaanza kumwambia Yakobo:[l] "Nipe watoto, kama sivyo nitakufa mimi."[m] **2** Kwa hiyo hasira ya Yakobo ikawaka juu ya Raheli naye akasema:[n] "Je, mimi niko badala ya Mungu, ambaye amekuzuilia uzao wa tumbo?"[o] **3** Basi yeye akasema: "Kijakazi wangu Bilha[a] huyu. Lala naye, apate kuzaa magotini pangu ili kwamba mimi, naam mimi, nipate watoto kwake."[b] **4** Basi akampa Bilha mjakazi wake awe mke na Yakobo akalala naye.[c] **5** Na Bilha akapata mimba na baada ya muda akamzalia Yakobo mwana.[d] **6** Ndipo Raheli akasema: "Mungu ametenda kama mwamuzi[e] wangu na pia ameisikiliza sauti yangu, akanipa mwana." Ndiyo sababu alimwita jina lake Dani.[f] **7** Na Bilha, mjakazi wa Raheli, akapata mimba mara nyingine tena, na baada ya muda akamzalia Yakobo mwana wa pili. **8** Kisha Raheli akasema: "Nimepigana miereka yenye ngu vu na dada yangu. Nami nimekuwa mshindi!" Kwa hiyo akamwita jina lake Naftali.[g]

9 Lea alipoona kwamba ameacha kuzaa, akamchukua Zilpa mjakazi wake akampa Yakobo kuwa mke.[h] **10** Baada ya muda Zilpa, mjakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana. **11** Ndipo Lea akasema: "Neema!" Basi akamwita jina lake Gadi.[i] **12** Baada ya hayo, Zilpa, mjakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana wa pili. **13** Kisha Lea akasema: "Pamoja na furaha yangu! Kwa maana binti watanitangaza kuwa mwenye furaha."[j] Basi akamwita jina lake Asheri.[k]

14 Ndipo Rubeni[l] akaenda kutembea siku za mavuno ya ngano,[m] akapata dudai shambani. Kwa hiyo akazileta kwa Lea mama yake. Kisha Raheli akamwambia Lea: "Tafadhali, nipe baadhi ya dudai za

SURA 29
a Mwa 30:3; Mwa 35:22
b Kum 21:15
c Ho 12:12
d Mwa 46:15; Ru 4:11
e Mwa 30:22
f Mwa 35:22; Mwa 37:22; Mwa 49:3; Kut 6:14; 1Nya 5:1; Ufu 7:5
g Mwa 30:20; 1Sa 1:6; Lu 1:25
h Mwa 30:6; Zb 34:15
i Mwa 34:25; Mwa 42:24; Mwa 49:5; 1Nya 4:24; Ufu 7:7
j Mwa 34:25; Mwa 49:5; Kut 6:16; Hes 3:12; 1Nya 6:1; Ufu 7:7
k Mwa 35:23; Mwa 37:26; Mwa 38:15; Mwa 44:18; Mwa 49:8; 1Nya 2:3; Ufu 5:5; Ufu 7:5

SURA 30
l Mwa 16:5; 1Sa 1:6; Met 14:30; Tit 3:3
m Hes 11:15; 1Sa 1:10; Yer 20:18
n Efe 4:26; Kol 3:19
o 1Sa 1:5; Zb 127:3; Ho 9:11

Safu ya 2
a Mwa 29:29
b Mwa 16:2; Mwa 50:23; Ru 4:17
c Mwa 22:24; Mwa 25:6; Mwa 35:22
d Mwa 16:15
e Amu 11:27; Zb 26:1; Zb 75:7
f Mwa 35:25; Mwa 46:23; Mwa 49:16
g Mwa 35:25; Mwa 46:24; Mwa 49:21; Kum 33:23; Ufu 7:6
h Mwa 35:26
i Mwa 49:19; Hes 32:33; Ufu 7:5
j Wim 6:9; Lu 1:48
k Mwa 35:26; Mwa 46:17; Mwa 49:20; Kum 33:24; Ufu 7:6
l Mwa 29:32
m Kut 34:22; Yoh 4:35.

mwana wako."[a] **15** Akajibu akamwambia: "Je, hili ni jambo dogo, kwamba wewe umemchukua mume wangu,[b] na sasa wewe uzichukue pia dudai za mwanangu?" Basi Raheli akasema: "Kwa sababu hiyo yeye atalala nawe usiku wa leo kwa kubadilishana na dudai za mwana wako."

16 Yakobo alipokuwa akitoka shambani jioni,[c] Lea akaenda kumpokea kisha akasema: "Utalala nami, kwa sababu nimekukodi moja kwa moja kwa dudai za mwanangu." Basi akalala naye usiku huo.[d] **17** Basi Mungu akamsikia na kumjibu Lea naye akapata mimba na baada ya muda akamzalia Yakobo mwana wa tano.[e] **18** Kisha Lea akasema: "Mungu amenipa mshahara wa mtu wa kukodiwa, kwa sababu nimempa mume wangu mjakazi wangu." Kwa hiyo akamwita jina lake Isakari.[f] **19** Lea akapata mimba mara nyingine tena na baada ya muda akamzalia Yakobo mwana wa sita.[g] **20** Ndipo Lea akasema: "Mungu amenipa kipawa, ndiyo, kipawa chema. Mwishowe mume wangu atanivumilia,[h] kwa sababu nimemzalia wana sita."[i] Basi akamwita jina lake Zabuloni.[j] **21** Na baadaye akazaa binti kisha akamwita jina lake Dina.[k]

22 Mwishowe Mungu akamkumbuka Raheli, naye Mungu akamsikia na kumjibu kwa kuwa alifungua tumbo lake la uzazi.[l] **23** Naye akapata mimba, akazaa mwana. Kisha akasema: "Mungu ameondolea mbali shutuma yangu!"[m] **24** Basi akamwita jina lake Yosefu,[n] akisema: "Yehova ananiongezea mwana mwingine."

SURA 30

a Wim 7:13
b Mwa 29:30
c Lu 2:8
d 1Ko 7:3
e Zb 65:2
Lu 1:13
f Mwa 35:23
Mwa 46:13
Mwa 49:14
Kum 33:18
1Nya 12:32
Ufu 7:7
g Ru 4:11
h Mwa 29:32
Zb 127:3
i Mwa 35:23
Mwa 46:15
j Mwa 46:14
Mwa 49:13
Kum 33:18
Ufu 7:8
k Mwa 34:1
l Mwa 29:31
1Sa 1:6
Zb 113:9
m Isa 54:1
Lu 1:25
n Mwa 35:24
Mwa 45:4
Kum 33:13
Mdo 7:9
Ufu 7:8

Safu ya 2

a Mwa 28:15
Mwa 31:13
b Mwa 31:41
Ho 12:12
c Mwa 12:3
Mwa 39:3
d Mwa 31:7
Law 19:13
e Mwa 31:38
Efe 6:8
f Zb 107:38
g Mwa 32:10
1Ti 5:8
h Zb 118:8
Ebr 13:5
i Mwa 46:34
Mwa 47:3
j 1Sa 25:7
Ho 12:12

25 Ikawa kwamba Raheli alipokuwa amemzaa Yosefu, bila kukawia Yakobo akamwambia Labani: "Niruhusu niende kwangu na katika nchi yangu.[a] **26** Nipe wake zangu na watoto wangu, ambao kwa ajili yao nimekutumikia, ili nipate kwenda; kwa maana wewe mwenyewe unajua utumishi wangu ambao nimekutolea."[b] **27** Ndipo Labani akamwambia: "Ikiwa, sasa, nimepata kibali machoni pako,—nimezifasiri zile ishara za bahati zinazoonyesha kwamba Yehova ananibariki kwa ajili yako."[c] **28** Naye akaongezea kusema: "Niambie masharti ya mshahara wako nami nitayatimiza."[d] **29** Basi akamwambia hivi: "Wewe mwenyewe unajua jinsi nimekutumikia na jinsi hali ya mifugo yako imekuwa mkononi mwangu;[e] **30** kwamba kwa kweli ulikuwa na kidogo kabla ya kuja kwangu, nayo ikaendelea kuongezeka na kuwa mingi, kwa kuwa Yehova alikubariki tangu nilipoingia.[f] Basi sasa ni wakati gani mimi nitafanya jambo pia kwa ajili ya nyumba yangu mwenyewe?"[g]

31 Kisha akasema: "Nikupe nini?" Naye Yakobo akaendelea kusema: "Hutanipa chochote kamwe![h] Ukinitendea jambo hili, mimi nitaanza tena kuchunga kundi lako.[i] Nitaendelea kulilinda.[j] **32** Mimi nitapita kati ya kundi lako lote leo. Wewe uweke kando kutoka hapo kila kondoo mwenye mabaka na mwenye madoa-doa ya rangi, na kila kondoo mwenye rangi ya kahawia kati ya wanakondoo dume na yeyote kati ya mbuzi-jike mwenye madoa-

doa ya rangi na mabaka. Baada ya hapo hao wawe mshahara wangu.[a] **33** Na wema wangu niliotenda utanitetea siku yoyote ya baadaye ambayo huenda ukaja kuutazama mshahara wangu;[b] kila mmoja asiye na mabaka na madoa-doa ya rangi kati ya mbuzi-jike na rangi ya kahawia kati ya wana-kondoo dume ni kitu kilichoibwa ikiwa yupo pamoja nami."[c]

34 Labani akajibu akasema: "Ni vema! Na iwe kulingana na neno lako."[d] **35** Kisha akaweka kando siku hiyo mbuzi-dume wenye mistari-mistari na madoa-doa ya rangi na mbuzi-jike wote wenye mabaka na madoa-doa ya rangi, kila mmoja kati ya wana-kondoo dume aliyekuwa na weupe wowote na kila mmoja wa rangi ya kahawia, lakini akawatia mikononi mwa wanawe. **36** Baada ya hayo akaenda kukaa umbali wa safari ya siku tatu kati yake na Yakobo, na Yakobo alikuwa akichunga mifugo ya Labani iliyobaki.

37 Kisha Yakobo akachukua fimbo zilizokuwa bado mbichi za mlubna[e] na za mlozi[f] na za mwaramoni ili azitumie,[g] akaziambua madoa meupe kwa kumenya sehemu nyeupe-nyeupe zilizokuwa kwenye hizo fimbo.[h] **38** Mwishowe zile fimbo alizokuwa amezimenya akaziweka mbele ya kundi, katika mifereji, katika vyombo vya kunyweshea wanyama,[i] ambapo makundi wangekuja kunywa, ili wapate kupandana mbele yazo walipokuja kunywa.

39 Basi hayo makundi yalikuwa yakipata hamu ya kupandana mbele ya hizo fimbo, nayo makundi yalikuwa yakizaa wenye mistari-mistari, wenye mabaka na wenye madoa-doa ya rangi.[a] **40** Naye Yakobo akatenganisha wale wana-kondoo dume kisha akageuza nyuso za makundi kuelekea wale wenye mistari-mistari na wote wa rangi ya kahawia kati ya makundi ya Labani. Halafu akaweka makundi yake mwenyewe peke yake wala hakuwaweka kando na mifugo ya Labani. **41** Ikawa sikuzote kwamba wakati wowote ambao makundi yenye nguvu[b] yalikuwa tayari kupandana, Yakobo alikuwa akiweka hizo fimbo katika michirizi[c] mbele ya macho ya makundi, ili wapate hamu ya kupandana kando ya hizo fimbo. **42** Lakini makundi hayo yalipoonyesha unyonge hakuyaweka hapo. Kwa hiyo wanyonge sikuzote wakawa wa Labani, lakini wenye nguvu wakawa wa Yakobo.[d]

43 Na huyo mwanamume akaendelea kuongezeka zaidi na zaidi, akawa na makundi makubwa na wajakazi na watumishi wanaume na ngamia na punda.[e]

31 Baadaye akasikia maneno ya wana wa Labani, wakisema: "Yakobo amechukua kila kitu kilichokuwa cha baba yetu; naye amekusanya mali hii yote kutoka kwa mali iliyokuwa ya baba."[f] **2** Wakati Yakobo alipokuwa akiutazama-tazama uso wa Labani, tazama haukuwa pamoja naye kama hapo zamani.[g] **3** Mwishowe Yehova akamwambia Yakobo: "Rudi kwenye nchi ya baba zako na kwa watu wa jamaa yako,[h] nami

SURA 30
a Mwa 31:7; Kum 24:15; 1Fa 5:6; Ayu 7:2; Yer 22:13; 1Ti 5:18
b Mal 3:5
c Kut 22:1
d Mwa 31:8
e Ho 4:13
f Hes 17:8; Mhu 12:5
g Eze 31:8
h Hes 21:18; Zek 11:7
i Mwa 24:20

Safu ya 2
a Mwa 31:10
b Ayu 39:4
c Kut 2:16
d Mwa 31:9; Mwa 32:5
e Mwa 32:5; Mwa 36:7

SURA 31
f Mwa 30:33; Mhu 4:4
g Mwa 30:27; 1Sa 18:9
h Mwa 28:15; Mwa 32:9; Mwa 35:27

nitaendelea kuwa pamoja
nawe."[a] **4** Kisha Yakobo aka-
tuma ujumbe Raheli na Lea
waitwe waje shambani kwenye
kundi lake, **5** naye akawaa-
mbia:
"Ninaona uso wa baba yenu,
kwamba yeye si yuleyule kunie-
lekea kama hapo zamani;[b] lakini
Mungu wa baba yangu amekuwa
pamoja nami.[c] **6** Nanyi wenye-
we mnajua kwa hakika kwamba
nimemtumikia baba yenu kwa
nguvu zangu zote.[d] **7** Baba
yenu amenichezea, naye ame-
badili mshahara wangu mara
kumi, lakini Mungu hakumru-
husu anidhuru.[e] **8** Ikiwa kwa
upande mmoja alisema, 'Wenye
mabaka watakuwa mshahara
wako,' ndipo kundi zima lili-
zaa wenye mabaka; lakini iki-
wa kwa upande mwingine ali-
sema, 'Wenye mistari-mista-
ri watakuwa mshahara wako,'
ndipo kundi zima lilizaa we-
nye mistari-mistari.[f] **9** Kwa
hiyo Mungu akazidi kuchukua
mifugo ya baba yenu na kuni-
pa mimi.[g] **10** Mwishowe ika-
wa kwamba kundi lilipokuwa
na hamu ya kupandana nikai-
nua macho yangu nikaona ma-
ono katika ndoto[h] na tazama,
mbuzi-dume wanaopanda ku-
ndi walikuwa wenye mistari-
mistari, wenye mabaka na ma-
doa-doa.[i] **11** Kisha malaika
wa Mungu wa kweli akania-
mbia katika ndoto, 'Yakobo!' ni-
kajibu nikasema, 'Mimi hapa.'[j]
12 Naye akaendelea kusema,
'Inua macho yako, tafadhali,
uone mbuzi-dume wote wana-
opanda kundi ni wenye mi-
stari-mistari, mabaka na ma-
doa-doa, kwa maana nimeona
yote ambayo Labani anakute-
ndea.[k] **13** Mimi ndimi Mungu
wa kweli wa Betheli,[a] ambapo
ulitia mafuta nguzo[b] na amba-
po uliniwekea nadhiri.[c] Basi
ondoka, toka katika nchi hii
urudi kwenye nchi ya kuzaliwa
kwako.'"[d]
14 Ndipo Raheli na Lea wa-
kajibu na kumwambia: "Je, ku-
ngali na fungu la urithi tena
kwa ajili yetu katika nyumba ya
baba yetu?[e] **15** Je, kwa kweli
sisi hatuonwi kuwa wageni
kwake kwa kuwa yeye ame-
tuuza, hivi kwamba anaende-
lea kula sikuzote kutokana
na pesa zilizotolewa kwa aji-
li yetu?[f] **16** Kwa maana utaji-
ri wote ambao Mungu amechu-
kua kutoka kwa baba yetu ni
wetu na wa watoto wetu.[g] Basi
sasa kila jambo ambalo Mungu
amekuambia, fanya."[h]
17 Kisha Yakobo akaondo-
ka, akawapandisha watoto
wake na wake zake juu ya nga-
mia;[i] **18** naye akaanza kupe-
leka mifugo yake yote na mali
zote ambazo alikuwa ameku-
sanya,[j] mifugo ya mapato yake
ambayo alikuwa amekusanya
Padan-aramu, ili aende kwa
Isaka baba yake katika nchi ya
Kanaani.[k]
19 Sasa Labani alikuwa
ameenda kunyoa kondoo wake.
Wakati huohuo Raheli aliiba
terafimu[l] zilizokuwa za baba
yake. **20** Kwa hiyo Yakobo
akamshinda akili Labani, Msi-
ria, kwa sababu hakuwa ame-
mwambia kwamba atakimbia.
21 Naye akakimbia, akaondo-
ka na kuvuka ule Mto,[m] yeye
na vyote alivyokuwa navyo.
Baada ya hapo akaelekeza uso
wake kwenye eneo lenye mi-
lima la Gileadi.[n] **22** Baadaye,
siku ya tatu, Labani aliambi-
wa kwamba Yakobo alikuwa

SURA 31
a Isa 41:10
Ro 8:31
Ebr 13:5
b Mwa 30:27
c Mwa 48:15
d Mwa 30:29
Efe 6:8
Kol 3:23
e Zb 37:28
Mhu 8:12
Isa 54:17
1Pe 3:13
f Mwa 30:32
g Met 13:22
h Hes 12:6
i Mwa 30:39
j Isa 6:8
k Mwa 29:25
Mwa 31:39
Kum 24:15

Safu ya 2
a Mwa 12:8
Mwa 35:15
b Mwa 28:18
Mwa 35:14
c Mwa 28:22
Kum 23:21
Mhu 5:4
d Mwa 37:1
e Hes 27:4
f Mwa 31:41
Ho 12:12
g Mwa 31:1
h Mwa 31:3
Mwa 32:9
Zb 45:10
i Mwa 33:13
j Mwa 30:43
k Mwa 35:27
l Mwa 31:14
Mwa 31:30
Mwa 35:2
Yos 24:2
Eze 21:21
Zek 10:2
m Mwa 15:18
n Hes 32:1

amekimbia. **23** Basi akachukua ndugu zake pamoja naye
akaanza kumfuatilia[a] mwendo
wa safari ya siku saba, akamfikia katika eneo lenye milima la Gileadi. **24** Ndipo Mungu akamjia Labani Msiria[b] katika ndoto wakati wa usiku[c] na kumwambia: "Jiangalie usije ukamwambia Yakobo jema wala baya."[d]

25 Basi Labani akamkaribia Yakobo, kwa kuwa Yakobo alikuwa amepiga hema mlimani na Labani alikuwa amepiga kambi kwa ajili ya ndugu zake katika eneo lenye milima la Gileadi. **26** Ndipo Labani akamwambia Yakobo: "Umefanya nini, kwa kuwa ulinishinda akili na kupeleka binti zangu kama mateka waliochukuliwa kwa upanga?[e] **27** Kwa nini ukakimbia kisiri na kunishinda akili wala usiniambie, ili nipate kukuaga kwa shangwe na kwa nyimbo,[f] kwa tari na kwa kinubi?[g] **28** Nawe hukunipa nafasi ya kuwabusu watoto wangu na binti zangu.[h] Basi umetenda kipumbavu. **29** Mkono wangu una nguvu za kuwatendea ninyi mabaya,[i] lakini Mungu wa baba yenu aliongea nami usiku uliopita, akisema, 'Jiangalie usije ukamwambia Yakobo jema wala baya.'[j] **30** Ingawa wewe kwa kweli umeenda sasa kwa sababu umekuwa ukitamani mno nyumba ya baba yako, hata hivyo, kwa nini umeiba miungu yangu?"[k]

31 Yakobo akajibu, akamwambia Labani: "Ni kwa sababu niliogopa.[l] Kwa maana nilisema moyoni mwangu, 'Unaweza kuninyang'anya binti zako.' **32** Yeyote yule ambaye huenda ukampata akiwa na miungu yako, asiishi.[a] Mbele ya ndugu zetu, chunguza mwenyewe kile kilicho pamoja nami na uichukue."[b] Lakini Yakobo hakujua kwamba Raheli alikuwa ameiiba.[c] **33** Kwa hiyo Labani akaingia katika hema la Yakobo na hema la Lea na hema la wale vijakazi wawili,[d] lakini hakuipata. Mwishowe akatoka katika hema la Lea akaenda katika hema la Raheli. **34** Basi Raheli alikuwa amechukua hizo terafimu, naye akaziweka katika kikapu cha matandiko ya kukaliwa na mwanamke juu ya ngamia, naye akaendelea kuzikalia. Basi Labani akakagua hema lote, lakini hakuzipata. **35** Ndipo Raheli akamwambia baba yake: "Hasira isiwake machoni pa bwana wangu,[e] kwa sababu mimi siwezi kusimama mbele yako, kwa maana nimepatwa na kilicho desturi kwa wanawake."[f] Kwa hiyo akaendelea kutafuta kwa uangalifu, lakini hakuzipata hizo terafimu.[g]

36 Naye Yakobo akakasirika,[h] akaanza ugomvi na Labani, na Yakobo akajibu na kumwambia Labani: "Kuna maasi gani upande wangu,[i] ni nini dhambi yangu, iwe ndiyo sababu umenifuatilia vikali?[j] **37** Sasa kwa kuwa umekagua mali zangu zote, kati ya mali zote za nyumba yako umepata nini?[k] Kiweke hapa mbele ya ndugu zangu na ndugu zako,[l] uwaache waamue kati yetu wawili.[m] **38** Miaka hii 20 nimekuwa pamoja nawe. Kondoojike zako na mbuzi-jike zako hawakutokwa na mimba,[n] na kondoo-dume wa kundi lako sikuwala kamwe. **39** Mnyama

SURA 31

a Zb 10:2
b Mwa 25:20
Kum 26:5
Ho 12:12
c Mwa 20:3
Mt 27:19
d Mwa 24:50
Hes 24:13
Zb 105:15
e Mwa 2:24
f Zb 98:5
g Kut 15:20
Ayu 21:12
Zb 149:3
h Mwa 31:55
i Zb 52:1
Yoh 19:10
j Mwa 31:7
Mwa 31:24
Mdo 5:39
k Mwa 31:19
Mwa 35:2
Amu 18:24
Isa 37:12
Mdo 19:26
1Ko 10:14
l Mwa 31:43

Safu ya 2

a Mwa 44:9
b Mwa 30:33
c Mwa 31:19
d Mwa 46:18
Mwa 46:25
e Mwa 18:12
Law 19:3
Efe 6:2
f Law 15:19
Eze 22:10
g Mwa 31:19
2Fa 23:24
Zek 10:2
h Mwa 30:2
Met 19:11
Efe 4:26
i 1Sa 24:11
Zb 59:3
j Omb 4:19
k Kut 22:8
l Mwa 13:8
m 1Sa 12:3
1Ti 5:19
n Mwa 30:27
Ayu 21:10

yeyote aliyeraruliwa vipande-
vipande sikukuletea.[a] Mimi
mwenyewe nililipa hasara
yake. Iwe mmoja aliibwa waka-
ti wa mchana au aliibwa wakati
wa usiku, wewe ulimtaka mko-
noni mwangu.[b] **40** Nimejio-
nea kwamba wakati wa mcha-
na joto limenimaliza nguvu, na
baridi wakati wa usiku, nao
usingizi wangu ulikimbia ma-
choni pangu.[c] **41** Nina jumla
ya miaka 20 nyumbani kwako.
Mimi nimekutumikia miaka 14
kwa ajili ya binti zako wawi-
li na miaka 6 kwa ajili ya ku-
ndi lako, nawe ulizidi kubadili
mshahara wangu mara kumi.[d]
42 Kama Mungu wa baba ya-
ngu,[e] Mungu wa Abrahamu na
aliye Hofu ya Isaka,[f] hangeku-
wa upande wangu, wewe unge-
niacha sasa niende zangu niki-
wa mikono mitupu. Taabu na
kazi ya mikono yangu Mungu
ameona, na kwa hiyo akakuka-
ripia usiku uliopita."[g]

43 Ndipo Labani akajibu,
akamwambia Yakobo: "Binti
hawa ni binti zangu na wa-
toto hawa ni watoto wangu na
kundi hili ni kundi langu, na
kila kitu unachokitazama ni
changu na cha binti zangu. Ni
nini ninachoweza kuwatendea
hawa leo au watoto wao ambao
wamezaa? **44** Na sasa, njoo
tufanye agano,[h] mimi na wewe,
nalo liwe ushahidi kati yangu
nawe."[i] **45** Basi Yakobo aka-
chukua jiwe, akalisimamisha
liwe nguzo.[j] **46** Kisha Yakobo
akawaambia ndugu zake: "Chu-
kueni mawe!" Nao wakachukua
mawe na kufanyiza rundo.[k] Baa-
da ya hayo wakala huko juu
ya hilo rundo. **47** Labani aka-
anza kuliita Yegar-sahadutha,
lakini Yakobo akaliita Galeedi.

SURA 31
a Kut 22:13
1Sa 17:34
b Met 29:7
Omb 3:36
c Mwa 47:9
Kol 3:23
d Mwa 31:7
e Mwa 28:13
Mwa 31:29
f Mwa 31:53
Isa 8:13
g Mwa 31:24
Zb 31:7
h Mwa 26:28
Ga 3:15
i Mwa 21:30
Yos 22:27
3Yo 12
j Mwa 28:18
k Yos 4:7
Yos 4:20
Yos 24:26

Safu ya 2
a Mwa 31:23
b 2Nya 16:9
Met 5:21
Met 15:3
c Mal 2:15
Kol 3:19
d Amu 11:10
1Sa 12:5
Mal 2:14
e Mwa 31:45
f Yos 4:6
g Mwa 17:7
Lu 20:37
h Yos 24:2
i Mwa 31:42
j Mwa 18:5
Zb 104:15
k Mwa 31:28
l Mwa 24:60
m Mwa 27:43
Mwa 28:2

SURA 32
n Zb 34:7
o Lu 2:13

48 Ndipo Labani akasema:
"Rundo hili ni ushahidi kati ya-
ngu na wewe leo." Hiyo ndiyo
sababu akaliita jina lake Gale-
edi,[a] **49** na Mnara wa Mli-
nzi, kwa sababu alisema: "Ye-
hova na alinde kati yangu na
wewe wakati tunapokuwa ha-
tuonani.[b] **50** Ukiwatesa binti
zangu[c] na ukichukua wake ku-
ongezea binti zangu, hakuna
mwanadamu aliye pamoja nasi.
Ona! Mungu ni shahidi kati ya-
ngu na wewe."[d] **51** Na Laba-
ni akaendelea kumwambia Ya-
kobo: "Tazama, hapa pana ru-
ndo na nguzo ndiyo hii hapa
ambayo nimesimamisha kati
yangu na wewe. **52** Rundo
hili ni ushahidi, na hii ngu-
zo ni kitu kinachotoa ushahi-
di,[e] kwamba mimi sitapita ru-
ndo hili kuja juu yako na kwa-
mba wewe hutapita rundo hili
na nguzo hii kuja juu yangu ku-
nidhuru.[f] **53** Acha mungu wa
Abrahamu[g] na mungu wa Na-
hori[h] ahukumu kati yetu, mu-
ngu wa baba yao." Lakini Ya-
kobo akaapa kwa Hofu ya baba
yake Isaka.[i]

54 Baada ya hayo Yakobo
akachinja dhabihu katika huo
mlima na kuwaalika ndugu
zake wale mkate.[j] Basi wakala
mkate na kukaa usiku huo mli-
mani. **55** Hata hivyo, Laba-
ni akaamka asubuhi na mape-
ma, akawabusu[k] watoto wake
na binti zake, akawabariki.[l] Ki-
sha Labani akaondoka akarudi
kwake.[m]

32 Naye Yakobo akaondoka
akaenda zake, na malai-
ka za Mungu sasa wakakutana
naye.[n] **2** Bila kukawia, Yako-
bo alipowaona akasema: "Hii ni
kambi ya Mungu!"[o] Kwa hiyo

akapaita mahali hapo Mahanaimu.[a]

3 Kisha Yakobo akatuma wajumbe[b] mbele yake kwenda kwa Esau ndugu yake kwenye nchi ya Seiri,[c] eneo la Edomu,[d] **4** naye akawaamuru, akisema: "Haya ndiyo ambayo mtamwambia bwana wangu,[e] Esau, 'Mtumishi wako Yakobo amesema hivi: "Nimekaa pamoja na Labani nikiwa mgeni kwa muda mrefu mpaka sasa.[f] **5** Nami nimekuja kuwa na ng'ombe na punda, kondoo, na watumishi wanaume na wajakazi,[g] nami ningependa kupeleka neno kumjulisha bwana wangu, ili nipate kibali machoni pako."'"[h]

6 Baada ya muda hao wajumbe wakarudi kwa Yakobo, wakisema: "Tulifika kwa ndugu yako Esau, naye pia yuko njiani akija kukupokea, na pamoja naye wanaume mia nne."[i] **7** Naye Yakobo akaogopa sana, akaanza kuhangaika.[j] Kwa hiyo akawagawanya watu waliokuwa pamoja naye kuwa kambi mbili, na makundi na ng'ombe na ngamia,[k] **8** naye akasema: "Esau akija na kushambulia kambi moja, basi bila shaka kambi moja itabaki iponyoke."[l]

9 Baada ya hayo Yakobo akasema: "Ee Mungu wa baba yangu Abrahamu na Mungu wa baba yangu Isaka,[m] Ee Yehova, wewe unayeniambia, 'Rudi kwenye nchi yako na kwa watu wa jamaa yako nami nitakutendea vema,'[n] **10** mimi sistahili fadhili zote zenye upendo na uaminifu wote ambao umemwonyesha mtumishi wako,[o] kwa maana nilivuka huu mto Yordani nikiwa na fimbo yangu tu na sasa nimekuwa kambi mbili.[a] **11** Nakuomba,[b] unikomboe kutoka katika mkono wa ndugu yangu, kutoka katika mkono wa Esau, kwa sababu mimi ninaogopa kwamba huenda akaja na kunishambulia,[c] mama pamoja na watoto. **12** Nawe, umesema, 'Bila shaka nitakutendea vema nami nitaufanya uzao wako uwe kama chembe za mchanga wa baharini, usioweza kuhesabika kwa sababu ya wingi wake.'"[d]

13 Naye akaendelea kukaa hapo usiku huo. Na kutoka katika kile kilichokuja kuwa mkononi mwake akachukua zawadi kwa ajili ya Esau ndugu yake:[e] **14** mbuzi-jike 200 na mbuzi-dume 20, kondoo-jike 200 na kondoo-dume 20, **15** ngamia 20 wanaonyonyesha na watoto wao, ng'ombe 40 na ng'ombe-dume 10, punda-jike 20 na punda 10 waliokomaa.[f]

16 Kisha akawapa watumishi wake kundi moja moja, kundi moja baada ya lingine na kwa kurudia-rudia akawaambia watumishi wake: "Vukeni mbele yangu, nanyi mnapaswa kuweka nafasi kati ya kundi na kundi."[g] **17** Tena akamwamuru yule wa kwanza, akisema: "Ikiwa Esau ndugu yangu atakupokea na kukuuliza, akisema, 'Wewe ni wa nani, nawe unaenda wapi na hawa walio mbele yako ni wa nani?' **18** ndipo utasema, 'Ni wa mtumishi wako, Yakobo. Ni zawadi,[h] iliyotumwa kwa bwana wangu,[i] Esau, na tazama! yeye mwenyewe yuko nyuma yetu pia.'" **19** Naye akamwamuru tena yule wa pili, na wa tatu

SURA 32

a 2Sa 17:24
Wim 6:13
b Lu 9:52
Lu 14:32
c Mwa 27:39
Mwa 36:8
Kum 2:5
Yos 24:4
d Mwa 25:30
Amu 5:4
e Mwa 23:6
Ro 12:10
f Mwa 31:41
g Mwa 30:43
Mwa 33:11
h Mwa 33:8
Mwa 47:25
i Mwa 33:1
j Mwa 27:41
Mwa 32:11
k Met 2:11
Mhu 9:18
l Mwa 33:1
m Kut 3:6
1Pe 5:7
n Mwa 31:3
Mwa 31:13
o Mwa 28:15
Zb 100:5
Mik 7:20

Safu ya 2

a Mwa 28:10
Mwa 30:43
Mwa 32:7
Zb 113:7
b Zb 34:4
Zb 107:19
2Pe 2:9
c Mwa 27:41
Zb 112:8
Met 18:19
d Mwa 28:14
Mwa 46:3
Kut 1:7
Kut 32:13
Mdo 7:17
e Mwa 33:10
Met 18:16
Ro 12:20
f Mwa 30:43
g Mwa 33:8
Mt 10:16
h Mwa 32:13
1Sa 25:27
i Mwa 33:8
Lu 14:32

pia, na wote wale wenye ku-
fuata hayo makundi pia, aki-
sema: "Kulingana na neno hili
ninyi mtasema na Esau mta-
kapokutana naye.[a] **20** Nanyi
pia mnapaswa kusema, 'Ta-
zama, mtumishi wako Yakobo
yuko nyuma yetu.'"[b] Kwa ma-
ana alisema moyoni mwake:
"Huenda nikamtuliza kwa za-
wadi inayoenda mbele yangu,[c]
na baadaye mimi nitaona uso
wake. Labda atanipokea kwa
fadhili."[d] **21** Kwa hiyo ile za-
wadi ikavushwa mbele yake,
lakini yeye mwenyewe akakaa
kambini usiku huo.[e]

22 Baadaye usiku huo akao-
ndoka, akachukua wake zake[f]
wawili na wajakazi[g] wake wa-
wili na wanawe[h] wachanga
kumi na mmoja akavuka kivu-
ko cha Yaboki.[i] **23** Basi aka-
wachukua, akawavusha bonde
la mto,[j] naye akavusha alivyo-
kuwa navyo.

24 Mwishowe Yakobo akaba-
ki peke yake. Ndipo mwana-
mume mmoja akaanza kupi-
gana mweleka pamoja naye
mpaka kulipopambazuka.[k]
25 Yeye alipoona kwamba ha-
kuwa amemshinda,[l] akagusa
tundu la fundo la paja lake;
nalo tundu la fundo la paja
la Yakobo likateguka waka-
ti wa kupigana naye mwele-
ka.[m] **26** Baada ya hayo aka-
sema; "Niache niende, kwa ma-
ana kumepambazuka." Naye
akajibu, akasema: "Mimi sita-
kuacha uende mpaka unibariki
kwanza."[n] **27** Kwa hiyo aka-
mwambia: "Jina lako ni nani?"
akajibu, akasema: "Yakobo."
28 Kisha akasema: "Hutaitwa
tena Yakobo bali Israeli,[o]
kwa maana wewe umeshinda-
na[p] na Mungu na wanadamu

SURA 32
a Met 13:17
b Met 25:13
c Mwa 43:11
1Sa 25:18
Met 17:8
d Zb 133:1
Met 6:3
e Mwa 32:13
f Mwa 29:30
Ru 4:11
g Mwa 30:3
Mwa 30:9
h Mwa 30:26
i Kum 3:16
Amu 11:13
j Yos 12:2
k Ho 12:3
l Ho 12:4
m Mwa 32:32
2Ko 12:7
n 1Nya 4:10
Zb 115:12
Ho 12:4
o Mwa 35:10
2Fa 17:34
Zb 22:23
Zb 78:71
p Ho 12:3

Safu ya 2
a Amu 13:18
b Amu 8:8
1Fa 12:25
c Mwa 16:7
Mwa 16:13
Amu 6:22
Yoh 1:18
d Mwa 32:25
e Ayu 10:11

SURA 33
f Mwa 14:14
Mwa 32:6
g Mwa 32:22
h Mwa 30:7
Mwa 30:12
i Mwa 30:19
j Mwa 30:22
k Met 6:3
Lu 14:11
l Mwa 27:44
m Mhu 3:5

hata ukashinda mwishowe."
29 Naye Yakobo akauliza na
kusema: "Tafadhali, niambie
jina lako." Lakini, yeye akase-
ma: "Kwa nini unauliza jina la-
ngu?"[a] Kisha akambariki huko.
30 Basi Yakobo akapaita ma-
hali hapo Penieli,[b] kwa saba-
bu, kama alivyosema, "Mimi ni-
memwona Mungu uso kwa uso
na bado nafsi yangu ikakombo-
lewa."[c]

31 Nalo jua likaanza kua-
ngaza juu yake mara tu alipo-
pita karibu na Penueli, naye
alikuwa akichechemea kwe-
nye paja lake.[d] **32** Ndiyo sa-
babu wana wa Israeli hawana
desturi ya kula kano ya mshi-
pa wa paja, ulio kwenye tundu
la fundo la paja, mpaka leo hii,
kwa sababu aligusa tundu la fu-
ndo la paja la Yakobo karibu na
kano ya mshipa wa paja.[e]

33 Baada ya muda Yako-
bo aliinua macho yake
akaona, na tazama, Esau ali-
kuwa anakuja na pamoja
naye walikuwa wanaume mia
nne.[f] Basi akagawanya wato-
to kwa Lea na kwa Raheli
na kwa wale wajakazi wawi-
li,[g] **2** naye akawaweka waja-
kazi na watoto wao kwanza ka-
bisa[h] na Lea na watoto wake
baada yao[i] na Raheli na Yosefu
nyuma yao.[j] **3** Naye mwenye-
we akapita mbele yao akaanza
kuinama mpaka chini mara
saba mpaka alipomkaribia ndu-
gu yake.[k]

4 Kisha Esau akaanza kuki-
mbia kwenda kumpokea.[l] Naye
akaanza kumkumbatia[m] na ku-
mwangukia shingoni, akambu-
su, nao wakatokwa na macho-
zi. **5** Kisha akainua macho
yake akaona wale wanawake

na wale watoto na kusema:
"Hawa walio pamoja nawe ni
nani?" naye akasema: "Wato-
to ambao Mungu amemkuba-
lia mtumishi wako kuwa nao."[a]
6 Ndipo wale wajakazi wakaja
mbele, wao pamoja na watoto
wao, wakainama chini; **7** na
Lea pia akaja mbele, na watoto
wake, nao wakainama chini, na
baadaye Yosefu akaja mbele, na
Raheli, nao wakainama chini.[b]
8 Ndipo yeye akasema:
"Unamaanisha nini kwa ka-
mbi yote hii ya wasafiri ambao
nimekutana nao?"[c] Naye aka-
jibu, akasema: "Kusudi nipate
kibali machoni pa bwana wa-
ngu."[d] **9** Kisha Esau akase-
ma: "Nina vitu vingi, ndugu ya-
ngu.[e] Vilivyo vyako na viende-
lee kuwa vyako." **10** Lakini
Yakobo akasema: "Hapana, ta-
fadhali. Ikiwa, sasa, nimepata
kibali machoni pako,[f] basi ichu-
kue zawadi yangu mkononi
mwangu, kwa sababu kwa ku-
patana na kusudi lake mimi
nimeona uso wako kana kwa-
mba ni kuona uso wa Mungu
kwa kuwa umenipokea vizuri.[g]
11 Tafadhali, ichukue zawa-
di ya baraka yangu iliyoletwa
kwako,[h] kwa sababu Mungu
amenipa kibali na kwa saba-
bu nina kila kitu."[i] Naye aka-
endelea kumhimiza, hata akai-
chukua.[j]
12 Baadaye Esau akasema:
"Na tuondoke twende, nami ni-
ende mbele yako." **13** Lakini
akamwambia: "Bwana wangu
anajua kwamba hawa watoto ni
dhaifu na kondoo na ng'ombe
wanaonyonyesha wako chini
ya usimamizi wangu.[k] Nao wa-
kiwaendesha haraka mno kwa
siku moja, basi kundi zima li-
takufa bila shaka.[l] **14** Tafa-
dhali, bwana wangu na apite
mbele ya mtumishi wake, la-
kini acha mimi mwenyewe ni-
endelee na safari kwa waka-
ti wangu kulingana na mwe-
ndo wa mifugo[a] walio mbele
yangu na kulingana na mwe-
ndo wa watoto[b] mpaka nimfi-
kie bwana wangu huko Seiri."[c]
15 Kisha Esau akasema: "Tafa-
dhali, acha niweke chini ya ma-
mlaka yako baadhi ya watu wa-
lio pamoja nami." Naye akaji-
bu, akasema: "Kwa nini hivyo?
Acha nipate kibali machoni pa
bwana wangu."[d] **16** Basi siku
hiyo Esau akageuka, akaenda
zake mpaka Seiri.
17 Naye Yakobo akaondoka
kuelekea Sukothi,[e] naye akaji-
jengea nyumba na kutengene-
za vibanda[f] kwa ajili ya mifugo
yake. Ndiyo sababu aliita jina la
mahali hapo Sukothi.
18 Baada ya muda Yakobo
akafika jiji la Shekemu[g] lililo
katika nchi ya Kanaani[h] aki-
wa salama salimini, alipoku-
wa akija kutoka Padan-ara-
mu,[i] naye akapiga kambi mbele
ya jiji hilo. **19** Kisha akajipa-
tia sehemu ya shamba alipo-
piga hema lake kutoka kwa
mkono wa wana wa Hamori
baba ya Shekemu, kwa vipande
mia moja vya pesa.[j] **20** Baa-
da ya hayo akasimamisha hapo
madhabahu, akaiita Mungu ali-
ye Mungu wa Israeli.[k]
34 Sasa Dina binti ya Lea,[l]
ambaye alimzalia Yako-
bo, alizoea kwenda nje kuwa-
ona[m] binti za nchi.[n] **2** Naye
Shekemu mwana wa Hamori
Mhivi,[o] mkuu wa nchi, aka-
mwona, kisha akamchukua,
akalala naye, akamnajisi.[p]
3 Nayo nafsi yake ikaanza

SURA 33
a Mwa 32:22
Zb 127:3
b Mwa 33:2
c Mwa 32:16
d Mwa 32:5
Mwa 33:15
Met 18:16
e Mwa 36:7
f Mwa 47:29
g Mwa 32:11
Mwa 32:20
Ayu 33:26
h Mwa 32:13
Met 18:16
i Mwa 30:43
Ebr 13:5
j Mdo 16:15
k Mwa 31:17
Isa 40:11
l Met 12:10

Safu ya 2
a Met 12:10
b Isa 40:11
Ro 15:1
c Mwa 27:39
Mwa 32:3
d Mwa 34:11
Ru 2:13
e Yos 13:27
1Fa 7:46
Zb 60:6
f Ebr 11:9
g Mwa 37:14
Yos 24:1
h Mwa 10:19
Mwa 12:6
i Mwa 25:20
Mwa 28:6
j Yos 24:32
Mdo 7:16
k Mwa 35:1
Mwa 35:7

SURA 34
l Mwa 30:21
Mwa 46:15
m 1Fa 11:2
1Ko 15:33
2Ko 6:14
n Mwa 26:35
Mwa 27:46
o Kum 7:1
1Nya 1:15
p Mwa 6:2
Mwa 34:26
Kum 22:29
2Sa 13:14
1Ko 6:18

kushikamana na Dina binti
ya Yakobo, naye akampenda
huyo mwanamke kijana, aka-
wa akiongea na huyo mwana-
mke kijana kwa kumshawishi.
4 Mwishowe Shekemu aka-
mwambia Hamori baba yake:[a]
"Nichukulie bibi huyu mcha-
nga awe mke wangu."[b]
5 Ndipo Yakobo akasikia ya
kwamba alikuwa amemnajisi
Dina binti yake. Nao wanawe
walikuwa na mifugo yake sha-
mbani;[c] naye Yakobo akakaa ki-
mya mpaka waingie.[d] **6** Baa-
daye Hamori, baba ya Sheke-
mu, akamwendea Yakobo ase-
me naye.[e] **7** Nao wana wa
Yakobo wakaingia kutoka sha-
mbani mara tu waliposikia juu
ya hilo; na hao wanaume wa-
kaumia hisia zao, wakakasi-
rika sana,[f] kwa sababu aliku-
wa amefanya upumbavu wenye
kufedhehesha juu ya Israeli
kwa kulala na binti ya Yakobo,[g]
wakati ambapo jambo kama
hilo halipasi kufanywa.[h]
8 Naye Hamori akasema
nao, na kuwaambia: "Nafsi ya
Shekemu mwanangu imeshi-
kamana na binti yenu.[i] Tafa-
dhali, mpeni awe mke wake.[j]
9 Nanyi mfanye mapatano ya
ndoa pamoja nasi.[k] Mtatupa
sisi binti zenu, nanyi mtajichu-
kulia binti zetu.[l] **10** Nanyi
mnaweza kukaa pamoja nasi,
nayo nchi itakuwa wazi kwenu.
Kaeni mfanye biashara humo
na kufanya makao humo."[m]
11 Kisha Shekemu akamwa-
mbia baba yake na ndugu zake:
"Acheni nipate kibali machoni
penu, na chochote mtakacho-
niambia nitawapa. **12** Onge-
zeni sana pesa na zawadi za
ndoa mnazonitoza,[n] nami niko
tayari kutoa kulingana na mta-

SURA 34

a Mwa 33:19
b Mwa 21:21
Amu 14:2
c Mwa 37:13
d Zb 39:1
Mhu 3:7
e Kum 7:3
Ne 13:25
f Zb 37:8
Yak 1:20
g Kum 22:21
2Sa 13:22
h Ebr 13:4
i Kum 21:11
j Kut 22:16
k Kut 34:12
Yos 23:12
Ezr 9:14
l Mwa 24:3
Kum 7:3
1Fa 11:2
1Ko 7:39
m Mwa 42:34
Lu 19:15
n Mwa 24:53
1Sa 18:25
Ho 3:2

Safu ya 2

a Met 6:18
Met 16:29
Met 26:26
Mk 7:22
b Mwa 17:12
Ro 4:11
c Mwa 17:10
Kut 12:48
d Met 4:24
e Mwa 33:19
Mwa 34:2
f Mwa 34:15
g Mik 7:4
h 1Sa 22:14
i Mwa 23:10
Ru 4:1
Zek 8:16
j Met 14:15
k Mwa 13:9
l Mwa 34:9
Kum 7:3
Ezr 9:1

kavyoniambia; ila tu nipeni
huyo mwanamke kijana awe
mke wangu."
13 Nao wana wa Yakobo wa-
kamjibu Shekemu na Hamo-
ri baba yake kwa udanganyifu,
kwa sababu alikuwa amemnaji-
si Dina dada yao.[a] **14** Nao wa-
kaendelea kuwaambia: "Sisi
hatuwezi kamwe kufanya ja-
mbo la namna hiyo, kumpa
mwanamume mwenye govi[b]
dada yetu, kwa sababu hilo ni
shutuma kwetu. **15** Ni kwa
sharti hili tu tunaweza kuwa-
pa kibali, kwamba ninyi muwe
kama sisi, kila mwanamume
wenu atahiriwe.[c] **16** Ndipo
tutakapowapa ninyi binti zetu,
na sisi kujichukulia binti zenu,
nasi tutakaa pamoja nanyi na
kuwa kundi moja la watu.[d]
17 Lakini msipotusikiliza na
kutahiriwa, basi tutamchukua
binti yetu twende zetu."
18 Nayo maneno yao yaka-
onekana kuwa mema macho-
ni pa Hamori na machoni pa
Shekemu, mwana wa Hamori.[e]
19 Naye huyo kijana hakuka-
wia kutimiza sharti hilo,[f] kwa
sababu alipendezwa na binti ya
Yakobo na yeye alikuwa ndi-
ye mwenye kuheshimika[g] zaidi
katika nyumba nzima ya baba
yake.[h]
20 Kwa hiyo Hamori na She-
kemu mwana wake wakaenda
kwenye lango la jiji lao, wakaa-
nza kuongea na wanaume wa jiji
lao,[i] wakisema: **21** "Wanau-
me hawa ni wapenda-amani
kutuelekea.[j] Basi acheni wa-
kae nchini na kufanya bia-
shara humo kwa kuwa nchi
hii ni pana kabisa mbele yao.[k]
Sisi tunaweza kujichukulia bi-
nti zao wawe wake zetu na bi-
nti zetu tunaweza kuwapa.[l]

22 Hata hivyo, wanaume hao
watatupa sisi kibali chao cha
kukaa pamoja nasi ili tuwe ku-
ndi moja la watu kwa sharti
hili tu, kwamba kila mwana-
mume wetu atahiriwe sawa na
wanavyotahiriwa.[a] **23** Ndipo
mali zao na utajiri wao na mi-
fugo yao yote, je, hazitakuwa
zetu?[b] Basi na tuwape kibali
chetu wapate kukaa pamoja
nasi."[c] **24** Kisha wote waliokuwa wakitoka nje kupitia lango la jiji lake wakamsikiliza Hamori na Shekemu mwana wake, na wanaume wote wakatahiriwa, wale wote wanaotoka nje kupitia lango la jiji lake.

25 Lakini ikawa kwamba
siku ya tatu walipokuwa wa-
kiumwa,[d] wale wana wawili
wa Yakobo, Simeoni na Lawi,[e]
ndugu za Dina,[f] wakachukua
kila mmoja wao upanga wake,
wakaenda bila kutazamiwa
kwenye jiji hilo na kumuua
kila mwanamume.[g] **26** Na wa-
kamuua Hamori na Shekemu
mwana wake kwa makali
ya upanga.[h] Kisha wakamchu-
kua Dina kutoka nyumbani
kwa Shekemu, wakatoka nje.[i]
27 Wale wana wengine wa Ya-
kobo wakawashambulia wana-
ume waliotiwa majeraha ya ku-
fisha na kulipora jiji, kwa sa-
babu walikuwa wamemnaji-
si dada yao.[j] **28** Makundi yao
na mifugo yao na punda zao
na kile kilichokuwa jijini na
kile kilichokuwa shambani
wakachukua.[k] **29** Na riziki
yao yote na watoto wao wote
waliokuwa wadogo na wake
zao wakawachukua mateka,
hivi kwamba wakapora vyote
vilivyokuwa katika nyumba
hizo.[l]

SURA 34
a Mwa 17:11
b Met 23:4
1Ti 6:9
c Zb 35:20
d Yos 5:8
e Mwa 49:5
f Mwa 46:15
g Mwa 49:6
Mwa 49:7
Zb 140:2
Mik 2:1
h 2Sa 2:26
i Mwa 34:2
j Mwa 34:2
k Hes 31:11
l Kum 2:35
Kum 20:14
Yos 8:2

Safu ya 2
a Mwa 49:5
b Kut 5:21
Met 11:17
c Kum 7:1
d 2Sa 13:32

SURA 35
e Mwa 28:19
Mwa 31:13
f Mwa 27:43
g Mwa 31:19
Kum 5:7
Yos 23:7
1Ko 10:14
h Kut 19:10
i Mwa 28:13
Zb 46:1
j Mwa 28:20
Mwa 31:42
Met 3:6
Isa 43:2
k Yos 24:23
1Yo 5:21
l Kum 7:25
m Kut 1:12
Kut 23:27
Kum 11:25
Yos 2:9
Zb 14:5
n Mwa 28:19

30 Basi Yakobo akawaa-
mbia Simeoni na Lawi:[a] "Mme-
fanya nitengwe kwa kunifanya
kuwa kitu chenye kunuka kwa
wakaaji wa nchi hii,[b] kwa Wa-
kanaani na Waperizi; wakati
mimi ni mdogo kwa hesabu,[c]
nao watakusanyika pamoja juu
yangu wanishambulie, nami ni-
taangamizwa, mimi na nyu-
mba yangu." **31** Nao wakaji-
bu, wakasema: "Je, yeyote ana-
paswa kumtendea dada yetu
kama kahaba?"[d]

35 Kisha Mungu akamwa-
mbia Yakobo: "Ondoka,
uende Betheli, ukakae huko,[e]
nawe umjengee madhabahu
Mungu wa kweli, aliyekutokea
ulipokuwa ukimkimbia Esau
ndugu yako."[f]

2 Basi Yakobo akawaambia
watu wa nyumba yake na wote
waliokuwa pamoja naye: "Io-
ndoleeni mbali miungu ya ki-
geni iliyo katikati yenu,[g] na-
nyi mjisafishe na kubadili nguo
zenu za kujitanda,[h] **3** kisha
tuondoke, twende Betheli. Na
huko nitamjengea madhaba-
hu Mungu wa kweli aliyenijibu
siku ya taabu[i] yangu kwa kuwa
alikuwa pamoja nami katika
njia niliyoiendea."[j] **4** Basi
wakampa Yakobo miungu yote
ya kigeni[k] iliyokuwa mikono-
ni mwao na vipuli vilivyoku-
wa masikioni mwao, naye Yako-
bo akaficha[l] chini ya ule mti
mkubwa uliokuwa karibu na
Shekemu.

5 Kisha wakasafiri, nao
watu wa majiji yaliyowazu-
nguka wakamwogopa Mungu,[m]
kwa hiyo hawakuwafuatilia
wana wa Yakobo. **6** Mwisho-
we Yakobo akafika Luzi,[n] kati-
ka nchi ya Kanaani, yaani,

Betheli, yeye na watu wote wa-
liokuwa pamoja naye. **7** Ki-
sha akajenga madhabahu huko.
Akaanza kupaita mahali hapo
El-betheli, kwa sababu Mungu
wa kweli alikuwa amejifu-
nua kwake mahali hapo alipo-
kuwa akimkimbia ndugu yake.[a]
8 Baadaye Debora[b] mwana-
mke mlezi wa Rebeka akafa,
akazikwa sehemu ya chini ya
Betheli chini ya mti mku-
bwa sana. Basi akauita Alon-ba-
kuthi.

9 Sasa Mungu akamtokea
Yakobo tena alipokuwa akito-
ka Padan-aramu,[c] akambariki.[d]
10 Na Mungu akamwambia:
"Jina lako ni Yakobo.[e] Hutae-
ndelea kuitwa Yakobo, bali uta-
itwa Israeli." Naye akaanza ku-
mwita Israeli.[f] **11** Tena Mu-
ngu akamwambia: "Mimi ni
Mungu Mweza-Yote.[g] Zaa uo-
ngezeke. Mataifa na kutaniko
la mataifa yatatoka ndani yako,
na wafalme watatoka viunoni
mwako.[h] **12** Nayo nchi[i] amba-
yo nimewapa Abrahamu na
Isaka, nitakupa wewe, na uzao[j]
wako baada yako." **13** Kisha
Mungu akapanda kutoka kwa-
ke katika mahali hapo alipoku-
wa amesema naye.[k]

14 Basi Yakobo akasimami-
sha nguzo katika mahali alipo-
kuwa amesema naye,[l] nguzo ya
mawe, naye akamimina to-
leo la kinywaji juu yake na
kumimina mafuta juu yake.[m]
15 Naye Yakobo akapaita Be-
theli.[n]

16 Kisha wakasafiri kutoka
Betheli. Nao walipokuwa mba-
li kiasi kabla ya kufika Efra-
thi,[o] Raheli akaanza kuzaa,
na mambo yalikuwa yakimwe-
ndea vibaya alipokuwa akizaa.[p]
17 Basi alipokuwa na shida wa-
kati wa kuzaa, yule mzalishaji
akamwambia: "Usiogope, kwa
maana utamzaa mwana huyu
pia."[a] **18** Basi nafsi[b] yake ili-
pokuwa ikitoka (kwa sababu
alikufa)[c] akamwita jina lake
Ben-oni; lakini baba yake aka-
mwita Benyamini.[d] **19** Kwa
hiyo Raheli akafa na kuzikwa
njiani kuelekea Efrathi, yaani,
Bethlehemu.[e] **20** Yakobo
akasimamisha nguzo juu ya ka-
buri lake. Hiyo ndiyo nguzo ya
kaburi la Raheli mpaka leo hii.[f]

21 Kisha Israeli akasafiri na
kupiga hema lake umbali fula-
ni ng'ambo ya mnara wa Ede-
ri.[g] **22** Pindi moja, Israeli ali-
pokuwa akikaa[h] katika nchi
hiyo, Rubeni alienda akalala na
Bilha suria wa baba yake, naye
Israeli akapata kusikia juu ya
hilo.[i]

Basi Yakobo alikuwa na wana
kumi na wawili. **23** Wana wa
Lea walikuwa Rubeni,[j] mzaliwa
wa kwanza wa Yakobo, na Si-
meoni na Lawi na Yuda na Isa-
kari na Zabuloni. **24** Wana
wa Raheli walikuwa Yosefu na
Benyamini. **25** Nao wana
wa Bilha, mjakazi wa Rahe-
li, walikuwa Dani na Naftali.
26 Nao wana wa Zilpa, mjaka-
zi wa Lea, walikuwa Gadi na
Asheri. Hawa ndio wana wa Ya-
kobo aliowazaa akiwa Padan-
aramu.

27 Mwishowe Yakobo akae-
nda kwa Isaka baba yake
huko Mamre,[k] huko Kiriath-
arba,[l] yaani, Hebroni, ambako
Abrahamu na Isaka pia waliku-
wa wamekaa wakiwa wageni.[m]
28 Nazo siku za Isaka zika-
wa miaka 180.[n] **29** Kisha Isa-
ka akakata pumzi, akafa, naye
akakusanywa kwa watu wake,
akiwa mzee na mwenye kuto-

SURA 35

a Mwa 28:22
b Mwa 24:59
c Mwa 25:20
d Ho 12:4
e Mwa 25:26
Mwa 27:36
f Mwa 32:28
1Fa 18:31
g Mwa 17:1
Kut 6:3
2Ko 6:18
Ufu 15:3
h Mwa 17:5
Mwa 48:4
Mk 15:32
Yoh 12:13
i Mwa 15:18
Kum 34:4
j Ga 3:16
k Amu 13:20
Lu 24:31
l Mwa 31:52
Amu 9:6
m Mwa 28:18
n Mwa 28:19
o Mwa 48:7
Mik 5:2
Mt 2:6
p Mwa 3:16

Safu ya 2

a Mwa 30:24
1Sa 4:20
b Mwa 2:7
c Zb 146:4
Mhu 9:5
d Mwa 46:21
Mwa 49:27
Kum 33:12
e Mwa 48:7
f 1Sa 10:2
g Mik 4:8
h Mwa 14:13
2Sa 7:6
i Mwa 49:4
Law 18:8
1Nya 5:1
1Ko 5:1
j Mwa 49:3
k Mwa 31:18
l Mwa 23:2
m Mwa 15:13
Kut 6:4
Kut 23:9
Mdo 7:6
Ebr 11:9
n Mwa 25:20
Mwa 25:26

sheka na siku,[a] na Esau na Yakobo wanawe wakamzika.[b]

36 Na hii ndiyo historia ya Esau, yaani, Edomu.[c]

2 Esau alitwaa wake zake kutoka kwa binti za Kanaani:[d] Ada[e] binti ya Eloni Mhiti[f] na Oholibama[g] binti ya Ana, mjukuu wa Sibeoni Mhivi, **3** na Basemathi[h] binti ya Ishmaeli, dada ya Nebayothi.[i]

4 Na Ada akamzalia Esau, Elifazi, naye Basemathi akamzaa Reueli.

5 naye Oholibama akazaa Yeushi na Yalamu na Kora.[j]

Hao ndio wana wa Esau ambao wake zake walimzalia katika nchi ya Kanaani. **6** Baada ya hayo Esau akachukua wake zake na wanawe na binti zake na nafsi zote za nyumba yake na mifugo yake na wanyama wake wengine wote na mali yake yote,[k] aliyokuwa amekusanya katika nchi ya Kanaani, naye akaenda nchi iliyo mbali kutoka kwa Yakobo ndugu yake,[l] **7** kwa sababu mali zao zilikuwa nyingi sana wasiweze kukaa pamoja na nchi ya kigeni waliyokuwa wakikaa haikuweza kuwatoshelezea mahitaji yao kwa sababu ya mifugo yao.[m] **8** Basi Esau akaanza kukaa katika eneo lenye milima la Seiri.[n] Esau ni Edomu.[o]

9 Nayo hii ndiyo historia ya Esau baba ya Edomu katika eneo lenye milima la Seiri.[p]

10 Haya ndiyo majina ya wana wa Esau: Elifazi mwana wa Ada, mke wa Esau; Reueli mwana wa Basemathi, mke wa Esau.[q]

11 Nao wana wa Elifazi walikuwa Temani,[r] Omari, Sefo, Gatamu, na Kenasi.[a] **12** Naye Timna[b] akawa suria wa Elifazi, mwana wa Esau. Baada ya muda akamzalia Elifazi, Amaleki.[c] Hao ndio wana wa Ada, mke wa Esau.

13 Hawa ndio wana wa Reueli: Nahathi na Zera, Shamma na Miza.[d] Hao ndio waliokuja kuwa wana wa Basemathi,[e] mke wa Esau.

14 Na hawa ndio waliokuja kuwa wana wa Oholibama binti ya Ana, mjukuu wa Sibeoni, mke wa Esau, kwa kuwa alimzalia Esau, Yeushi na Yalamu na Kora.[f]

15 Hawa ndio mashehe[g] wa wana wa Esau: Wana wa Elifazi, mzaliwa wa kwanza wa Esau: Shehe Temani,[h] shehe Omari, shehe Sefo, shehe Kenasi, **16** shehe Kora, shehe Gatamu, shehe Amaleki. Hao ndio mashehe wa Elifazi[i] katika nchi ya Edomu. Hao ndio wana waliozaliwa na Ada.

17 Hawa ndio wana wa Reueli, mwana wa Esau: Shehe Nahathi, shehe Zera, shehe Shamma, shehe Miza. Hao ndio mashehe wa Reueli katika nchi ya Edomu.[j] Hao ndio wana waliozaliwa na Basemathi, mke wa Esau.

18 Na mwisho hawa ndio wana wa Oholibama, mke wa Esau: Shehe Yeushi, shehe Yalamu, shehe Kora. Hao ndio mashehe wa Oholibama binti ya Ana, mke wa Esau.

19 Hao ndio wana wa Esau, na hao ndio mashehe wao. Yeye ni Edomu.[k]

20 Hawa ndio wana wa Seiri, yule Mhori, wakaaji wa nchi hiyo:[l] Lotani na Shobali na Sibeoni na Ana[m] **21** na

SURA 35
a Mwa 25:8
1Nya 29:28
b Mwa 49:31

SURA 36
c Mwa 25:30
Kum 23:7
Eze 25:12
Ro 9:13
d Kum 7:3
Kum 9:5
Amu 3:5
e Mwa 36:10
f Mwa 26:34
g Mwa 36:18
h Mwa 36:17
i Mwa 25:13
Mwa 28:9
j 1Nya 1:35
k Mwa 33:9
Oba 6
l Mwa 27:39
Mwa 32:3
m Mwa 13:6
Mwa 28:4
n Mwa 14:6
Kum 2:5
o Mwa 25:30
p Kum 2:12
Oba 8
q 1Nya 1:35
r Mwa 36:34
Eze 25:13
Oba 9

Safu ya 2
a Mwa 36:42
1Nya 1:36
b 1Nya 1:39
c Kut 17:8
Hes 13:29
Hes 24:20
Kum 25:19
1Sa 15:8
1Sa 30:1
d 1Nya 1:37
e Mwa 26:34
f 1Nya 1:35
g Kut 15:15
h 1Nya 1:53
Ayu 4:1
Yer 49:20
i 1Nya 1:36
j Hes 20:23
Amu 11:18
1Fa 9:26
k Mwa 25:30
Mwa 32:3
Mal 1:3
l Mwa 14:6
Kum 2:12
Kum 2:22
m 1Nya 1:40

Dishoni na Ezeri na Dishani.[a] Hao ndio mashehe wa yule
Mhori, wana wa Seiri, katika
nchi ya Edomu.
22 Nao wana wa Lotani
wakawa Hori na Hemamu;
na dada ya Lotani alikuwa
Timna.[b]
23 Nao hawa ndio wana wa
Shobali: Alvani na Manahathi
na Ebali, Shefo na Onamu.
24 Nao hawa ndio wana wa
Sibeoni: Aya na Ana. Huyu
ndiye Ana aliyepata bubujiko
la maji ya moto nyikani alipo-
kuwa akiwachunga punda wa
Sibeoni baba yake.[c]
25 Nao hawa ndio watoto
wa Ana: Dishoni na Oholiba-
ma binti ya Ana.
26 Nao hawa ndio wana wa
Dishoni: Hemdani na Eshbani
na Ithrani na Kerani.[d]
27 Hawa ndio wana wa
Ezeri: Bilhani na Zaavani na
Akani.
28 Hawa ndio wana wa Di-
shani: Usi na Arani.[e]
29 Hawa ndio mashehe wa
yule Mhori: Shehe Lotani, she-
he Shobali, shehe Sibeoni, she-
he Ana, **30** shehe Dishoni,
shehe Ezeri, shehe Dishani.[f]
Hao ndio mashehe wa yule
Mhori kulingana na mashehe
wao katika nchi ya Seiri.
31 Sasa hawa ndio wafalme
waliotawala katika nchi ya
Edomu[g] kabla ya mfalme yeyo-
te kuwatawala wana wa Israe-
li.[h] **32** Naye Bela mwana wa
Beori akatawala Edomu,[i] na
jina la jiji lake lilikuwa Dinha-
ba. **33** Na Bela alipokufa, Yo-
babu mwana wa Zera kutoka
Bosra[j] akaanza kutawala ba-
dala yake.[k] **34** Yobabu alipo-
kufa, Hushamu kutoka katika
nchi ya Watemani[a] akaanza ku-
tawala badala yake.[b] **35** Hu-
shamu alipokufa, Hadadi mwa-
na wa Bedadi, aliyewashinda
Wamidiani[c] katika nchi ya Mo-
abu,[d] akaanza kutawala badala
yake, nalo jina la jiji lake lili-
kuwa Avithi.[e] **36** Hadadi ali-
pokufa, Samla kutoka Mas-
reka akaanza kutawala bada-
la yake.[f] **37** Samla alipokufa,
Shauli kutoka Rehobothi ka-
ndo ya ule Mto akaanza kuta-
wala badala yake.[g] **38** Shauli
alipokufa, Baal-hanani mwana
wa Akbori akaanza kutawala
badala yake.[h] **39** Baal-hanani
mwana wa Akbori alipokufa,
Hadari akaanza kutawala ba-
dala yake; na jina la jiji lake li-
likuwa Pau, nalo jina la mke
wake lilikuwa Mehetabeli binti
ya Matredi binti ya Mezahabu.[i]
40 Basi haya ndiyo majina ya
mashehe wa Esau kulingana na
familia zao, kulingana na ma-
hali pao, kwa majina yao: She-
he Timna, shehe Alva, she-
he Yethethi,[j] **41** shehe Oholi-
bama, shehe Ela, shehe Pinoni,[k]
42 shehe Kenasi, shehe Tema-
ni, shehe Mibsari,[l] **43** shehe
Magdieli, shehe Iramu. Hao
ndio mashehe wa Edomu[m] ku-
lingana na makao yao kati-
ka nchi yao.[n] Huyu ndiye Esau
baba ya Edomu.[o]

37 Naye Yakobo akaende-
lea kukaa katika nchi ya
kigeni ya baba yake,[p] katika
nchi ya Kanaani.[q]
2 Hii ndiyo historia ya Ya-
kobo.
Yosefu,[r] alipokuwa na umri
wa miaka kumi na saba, aliku-
wa akichunga kondoo pamoja
na ndugu zake kati ya kundi,[s]
na, kwa kuwa alikuwa mvula-

SURA 36
a 1Nya 1:38
b 1Nya 1:39
c Mwa 36:2
d 1Nya 1:41
e 1Nya 1:42
f 1Nya 1:38
g Hes 20:14
h Kum 17:14
Kum 17:15
1Sa 10:19
i 1Nya 1:43
j Isa 34:6
Yer 49:13
k 1Nya 1:44

Safu ya 2
a Ayu 2:11
b 1Nya 1:45
c Mwa 25:2
Kut 2:15
Hes 31:2
d Ru 1:1
e 1Nya 1:46
f 1Nya 1:47
g 1Nya 1:48
h 1Nya 1:49
i 1Nya 1:50
j 1Nya 1:51
k 1Nya 1:52
l 1Nya 1:53
m 1Nya 1:54
n Kum 2:5
o Mwa 25:30
Mwa 36:8

SURA 37
p Mwa 23:4
Mwa 28:4
Ebr 11:9
q Mwa 17:8
r Mwa 30:25
Mwa 46:19
s Mwa 47:3

na tu, alikuwa pamoja na wana
wa Bilha[a] na wana wa Zilpa,[b]
wake za baba yake. Basi Yose-
fu akamletea baba yake habari
mbaya juu yao.[c] **3** Naye Isra-
eli alimpenda Yosefu kuliko wa-
nawe wengine wote,[d] kwa saba-
bu alikuwa mwana wa uzee
wake; naye alikuwa amemsho-
nea vazi refu lenye mistari lina-
lofanana na shati.[e] **4** Ndugu
zake walipoona kwamba baba
yao alimpenda kuliko ndugu
zake wote, wakaanza kumchu-
kia,[f] nao hawakusema naye
kwa amani.[g]

5 Baada ya muda Yosefu ali-
ota ndoto, akawasimulia ndugu
zake,[h] nao wakawa na sababu
zaidi ya kumchukia. **6** Ali-
waambia hivi: "Tafadhali, si-
kilizeni ndoto hii ambayo ni-
meota.[i] **7** Tazama, tulikuwa
tukifunga miganda katikati
ya shamba wakati ambapo ta-
zama, mganda wangu uliinu-
ka, ukasimama wima nayo mi-
ganda yenu ikauzunguka na
kuuinamia mganda wangu."[j]
8 Nao ndugu zake wakamwa-
mbia: "Je, kwa kweli utakuwa
mfalme juu yetu?[k] Au utatuta-
wala?"[l] Basi wakapata sababu
mpya ya kumchukia kwa saba-
bu ya ndoto zake na maneno
yake.

9 Baadaye akaota ndoto nyi-
ngine tena, akawasimulia ndu-
gu zake na kusema: "Tazama
nimeota ndoto tena, na taza-
ma, jua na mwezi na nyota
kumi na moja zilikuwa zikinii-
namia."[m] **10** Kisha akamsi-
mulia baba yake na ndugu zake
vilevile, na baba yake akamke-
mea na kumwambia:[n] "Ndoto
hii ambayo umeota inamaani-
sha nini? Je, mimi na pia mama
yako na ndugu zako kwa kwe-
li tutakuja na kukuinamia?"
11 Na ndugu zake wakaanza
kumwonea wivu,[a] lakini baba
yake akayatia moyoni maneno
hayo.[b]

12 Sasa ndugu zake wakae-
nda kulisha kundi la baba yao
karibu na Shekemu.[c] **13** Ba-
ada ya muda, Israeli akamwa-
mbia Yosefu: "Je, ndugu zako
hawachungi makundi karibu
na Shekemu? Njoo, nikutu-
me kwao." Basi akamjibu,
akamwambia: "Mimi hapa!"[d]
14 Basi akamwambia: "Tafa-
dhali, nenda. Kaone kama ndu-
gu zako wako salama salimini
na kama kundi liko salama sali-
mini, halafu uniletee habari."[e]
Basi akamtuma toka nchi ta-
mbarare ya chini ya Hebroni,[f]
naye akaenda kuelekea She-
kemu. **15** Baadaye mwana-
mume fulani akamkuta na ta-
zama, alikuwa akizunguka-zu-
nguka shambani. Basi mwa-
namume huyo akamuuliza:
"Unatafuta nini?" **16** Akaji-
bu: "Nawatafuta ndugu zangu.
Tafadhali, niambie, Wanachu-
nga makundi wapi?" **17** Naye
mwanamume huyo akamwa-
mbia: "Wameondoka hapa,
kwa sababu niliwasikia wakise-
ma, 'Twendeni Dothani.'" Kwa
hiyo akaendelea kuwafuata
ndugu zake, akawapata huko
Dothani.

18 Ndugu zake wakamwo-
na akiwa mbali, na kabla ha-
jakaribia wakaanza kumpa-
ngia kwa ujanja hila ya kumu-
ua.[g] **19** Basi wakasemezana:
"Tazama! Yule mwota-ndoto
anakuja.[h] **20** Basi na tumu-
ue, tumtupe ndani ya moja
la mashimo ya maji;[i] halafu
tutasema mnyama mkali wa
mwitu alimrarua.[j] Ndipo tuone

SURA 37

a Mwa 35:25
b Mwa 35:26
c Law 5:1
1Sa 2:24
Yoh 7:7
d 1Nya 2:1
e Mwa 37:32
f Met 14:30
Met 27:4
g Ga 5:20
Tit 3:3
h Mwa 37:19
i Hes 12:6
j Mwa 42:6
Mwa 42:9
k Mwa 45:8
l Mwa 49:26
m Mwa 44:14
Mwa 45:9
n Met 17:10
Mhu 7:5

Safu ya 2

a Met 14:30
Mdo 7:9
Yak 3:14
b Da 7:28
Lu 2:19
c Mwa 33:18
d 1Sa 3:4
Isa 6:8
e 1Sa 17:17
Met 15:30
f Mwa 23:19
Mwa 35:27
g Zb 37:14
Zb 94:21
Met 6:17
Mt 15:19
h Mwa 37:5
i Zb 64:5
Met 1:11
Met 27:4
j Mwa 31:39
Kut 22:13

itakuwaje kwa ndoto zake.”
21 Rubeni aliposikia hilo alijaribu kumwokoa kutoka mikononi mwao.[a] Kwa hiyo akasema: “Tusiipige nafsi yake kiasi cha kuiua.”[b] **22** Naye Rubeni akaendelea kuwaambia: “Msimwage damu.[c] Mtupeni ndani ya shimo hili la maji lililo nyikani wala msimtendee kwa jeuri.”[d] Alikusudia kumwokoa kutoka katika mikono yao ili amrudishe kwa baba yake.

23 Basi mara tu Yosefu alipowafikia ndugu zake, wakamvua Yosefu vazi lake refu, naam, lile vazi refu lenye mistari alilokuwa amevaa;[e] **24** kisha wakamchukua na kumtupa ndani ya hilo shimo la maji.[f] Wakati huo shimo hilo lilikuwa tupu; halikuwa na maji ndani yake.

25 Kisha wakaketi ili kula mkate.[g] Walipoinua macho yao na kutazama, kumbe, kulikuwa na msafara wa Waishmaeli[h] uliokuwa ukija kutoka Gileadi, na ngamia zao walikuwa wamebeba ubani mweusi na zeri na gome lenye utomvu,[i] wakiwa njiani kuzipeleka Misri. **26** Basi Yuda akawaambia ndugu zake: “Kungekuwa faida gani tukimuua ndugu yetu na kufunika damu yake?[j] **27** Njooni, na tumuuze kwa Waishmaeli,[k] nasi tusiinue mkono wetu juu yake.[l] Bado yeye ni ndugu yetu, nyama yetu.” Kwa hiyo wakamsikiliza ndugu yao.[m] **28** Wanaume, wanabiashara Wamidiani,[n] wakapitia hapo. Basi wakamvuta na kumpandisha Yosefu kutoka katika lile shimo la maji[o] kisha wakamuuza kwa wale Waishmaeli kwa vipande 20 vya fedha.[p] Mwishowe wanabiashara hao wakampeleka Yosefu Misri.

29 Baadaye Rubeni akarudi kwenye lile shimo la maji na tazama Yosefu hakuwemo. Basi akayararua mavazi yake.[a] **30** Aliporudi kwa wale ndugu zake wengine akasema: “Mtoto hayuko! Na mimi—mimi kwa kweli nitaenda wapi?”[b]

31 Hata hivyo, wakalichukua lile vazi refu la Yosefu, wakamchinja mbuzi-dume na kulichovya-chovya vazi hilo katika damu.[c] **32** Kisha wakalipeleka lile vazi refu lenye mistari kwa baba yao na kusema: “Hiki ndicho tulichopata. Tafadhali, chunguza[d] kama ni lile vazi refu la mwana wako au hapana.”[e] **33** Naye akalichunguza na kusema: “Ni vazi la mwanangu! Mnyama-mwitu mkali amemrarua![f] Hakika Yosefu amararuliwa vipande-vipande!”[g] **34** Basi Yakobo akararua nguo zake za kujitanda, akavaa nguo za magunia viunoni mwake, akamwombolezea mwana wake siku nyingi.[h] **35** Nao wanawe wote na binti zake wote wakawa wakiondoka ili kumfariji,[i] lakini akawa akizidi kukataa kufarijiwa na kusema:[j] “Kwa maana nitashuka kuingia katika Kaburi* nikimwombolezea mwanangu!” Na baba yake akaendelea kumlilia.

36 Hata hivyo, Wamidiani wakamuuza Misri kwa Potifa, ofisa wa makao ya Farao,[k] mkuu wa walinzi.[l]

38 Sasa ikawa wakati huo kwamba Yuda aliposhuka kutoka kwa ndugu zake, alipiga hema karibu na mwa-

SURA 37

a Zb 97:10
Da 3:17
b Mwa 9:5
Kut 20:13
Law 24:17
1Yo 3:15
c Mwa 4:10
Mwa 42:22
Met 6:17
d Mwa 42:21
Zb 37:8
Yer 22:3
e Mwa 37:3
f Zb 69:8
g Amo 6:6
h Mwa 25:12
i Mwa 43:11
Kut 25:6
j Mwa 4:10
Kut 21:14
k Kut 21:16
Ne 5:8
Mdo 7:9
l Yer 22:3
m Met 12:15
n Mwa 25:2
o Yer 38:13
p Mwa 40:15
Mwa 45:4
Kum 24:7
Zb 105:17

Safu ya 2

a Mwa 44:13
Mdo 14:14
b Mwa 49:3
c Met 28:17
d Mwa 38:25
Hes 35:24
e Mwa 37:3
1Ti 5:24
f Mwa 44:28
g Kut 22:13
2Fa 2:24
h 2Sa 1:11
Ayu 1:20
i 1Th 5:14
j Zb 77:2
Mt 2:18
k Mwa 39:1
l Mwa 40:3

Mwa 37:35* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

namume, Mwadulamu,[a] na jina
lake lilikuwa Hira. **2** Na
huko Yuda akamwona binti
ya Mkanaani[b] fulani aliyekuwa
akiitwa Shua. Basi akamchu-
kua, akalala naye. **3** Naye
akapata mimba. Baadaye aka-
zaa mwana, akamwita jina lake
Eri.[c] **4** Akapata mimba tena.
Akazaa mwana, akamwita jina
lake Onani. **5** Tena akazaa
mwana, akamwita jina lake
Shela. Alipomzaa, Yuda aliku-
wa Akzibu.[d]

6 Baada ya muda Yuda aka-
mchukulia Eri mzaliwa wake
wa kwanza mke. Na mke huyo
aliitwa Tamari.[e] **7** Lakini
Eri, mzaliwa wa kwanza wa
Yuda, alikuwa mbaya macho-
ni pa Yehova;[f] kwa hiyo Yehova
akamuua.[g] **8** Basi Yuda aka-
mwambia Onani: "Lala na mke
wa ndugu yako, ufanye ndoa
ya ndugu-mkwe pamoja naye
umwinulie uzao ndugu yako."[h]
9 Lakini Onani alijua kwamba
uzao huo haungekuwa wake;[i]
basi alipolala na mke wa ndu-
gu yake akamwaga chini sha-
hawa zake ili asimpe ndugu
yake uzao.[j] **10** Sasa jambo ali-
lofanya lilikuwa baya machoni
pa Yehova;[k] kwa hiyo akamuua
yeye pia.[l] **11** Basi Yuda aka-
mwambia Tamari binti-mkwe
wake: "Kaa ukiwa mjane katika
nyumba ya baba yako mpa-
ka Shela mwanangu akue."[m]
Kwa maana alisema moyoni
mwake: "Huenda yeye pia aka-
fa kama ndugu zake."[n] Basi Ta-
mari akaenda, naye akaende-
lea kukaa katika nyumba ya
baba yake.[o]

12 Basi siku zikawa nyingi
naye binti ya Shua, mke wa
Yuda,[p] akafa; naye Yuda aka-
shika kile kipindi cha kuombo-
leza.[a] Kisha akaenda kwa wa-
nyoaji wa kondoo zake huko
Timna,[b] yeye na mwenzake,
Hira, Mwadulamu.[c] **13** Ndipo
Tamari akaambiwa: "Tazama
baba-mkwe wako anaenda Ti-
mna kuwanyoa kondoo zake."[d]
14 Basi akayavua mavazi ya
ujane wake, akavaa shali na
kujifunika uso, naye akake-
ti chini kwenye mwingilio wa
Enaimu, jiji lililo katika bara-
bara inayokwenda Timna. Kwa
maana aliona ya kwamba She-
la alikuwa ameshakuwa mtu
mzima na bado hakuwa ameka-
bidhiwa kwake awe mke wake.[e]

15 Mara Yuda alipomwona,
akamfikiria kuwa ni kahaba,[f]
kwa sababu alikuwa ameufu-
nika uso wake.[g] **16** Basi aka-
mwendea kando ya barabara
akamwambia: "Tafadhali, niru-
husu nilale nawe."[h] Kwa kuwa
hakujua kwamba alikuwa bi-
nti-mkwe wake.[i] Hata hivyo,
akasema: "Utanipa nini ili ulale
nami?"[j] **17** Akasema: "Mimi
mwenyewe nitakuletea mwa-
na-mbuzi kutoka katika ku-
ndi." Lakini akasema: "Je, uta-
toa rehani mpaka utakapomle-
ta?"[k] **18** Naye akasema: "Ni
rehani gani nitakayokupa?"
akasema: "Pete yako ya muhuri[l]
na kamba yako na fimbo
yako iliyo mkononi mwako."
Basi akampa vitu hivyo, akala-
la naye, naye akapata mimba.
19 Kisha akaondoka, akaenda,
akaivua ile shali na kuvaa ma-
vazi ya ujane wake.[m]

20 Na Yuda akamtuma mwe-
nzake Mwadulamu[n] ampele-
ke mwana-mbuzi ili arudishi-
we rehani kutoka mkononi mwa
yule mwanamke, lakini haku-
mpata kamwe. **21** Akawauliz-
a-uliza watu wa mahali pake,

SURA 38

a Yos 12:15
1Sa 22:1
b Mwa 24:3
Mwa 28:1
c Hes 26:19
d Yos 19:29
Amu 1:31
e Mt 1:3
f Kum 21:20
Ga 5:19
1Pe 3:12
g 2Sa 6:7
Mdo 12:23
h Kum 25:5
Kum 25:6
Ru 1:11
Mt 22:24
i Ru 4:6
j Kum 25:9
k Isa 65:12
l 1Nya 2:3
Zb 55:23
m Ru 1:13
Mt 22:24
n Hes 26:19
o Law 22:13
p Mwa 38:2

Safu ya 2

a Hes 20:29
Kum 34:8
b Yos 15:10
Amu 14:1
c Mwa 38:1
d 1Sa 25:4
e Kum 25:5
Ru 1:11
Mt 22:24
f Yer 3:2
g Met 7:10
h 1Ko 6:18
Ebr 13:4
i Mwa 38:11
j Kum 23:18
Eze 16:33
Lu 15:30
k Met 20:16
l Mwa 41:42
1Fa 21:8
Est 8:8
Da 6:17
m 2Sa 14:2
n Mwa 38:1

akisema: "Yuko wapi yule kahaba wa hekaluni katika Enaimu kando ya barabara?" Lakini wakawa wakisema: "Hakujawahi kuwa na kahaba wa hekaluni[a] mahali hapa." **22** Mwishowe akarudi kwa Yuda na kumwambia: "Sikumpata kamwe, tena, watu wa mahali hapo walisema, 'Hakujawahi kuwa na kahaba wa hekaluni mahali hapa.'" **23** Basi Yuda akasema: "Mwache avichukue viwe vyake, tusije tukadharaulika.[b] Tena, nimemtumia mwana-mbuzi huyu, lakini wewe hukumpata kamwe."

24 Hata hivyo, miezi mitatu hivi baadaye Yuda akaambiwa: "Tamari binti-mkwe wako amefanya ukahaba,[c] na tazama ana mimba[d] pia kutokana na ukahaba wake." Ndipo Yuda akasema: "Mtoeni nje ateketezwe."[e] **25** Alipokuwa akitolewa nje, akapeleka ujumbe kwa baba-mkwe wake, akisema: "Nina mimba ya mwanamume mwenye vitu hivi."[f] Naye akaongezea: "Tafadhali, vichunguze[g] ni vya nani, pete ya muhuri na kamba na fimbo."[h] **26** Basi Yuda akavichunguza na kusema:[i] "Yeye ni mwadilifu kuliko mimi,[j] kwa sababu sikumpa Shela mwanangu awe mke wake."[k] Naye hakulala naye tena baada ya hayo.[l]

27 Sasa ilitukia kwamba wakati wake wa kuzaa ulipofika, tazama, kulikuwa na mapacha tumboni mwake. **28** Tena, alipokuwa akizaa mmoja akaunyoosha mkono wake, na mara moja mzalishaji akamfunga kitambaa chekundu mkononi, akisema: "Huyu alitoka kwanza." **29** Mwishowe ikatokea kwamba mara tu alipourudisha mkono wake, tazama ndugu yake akatoka. Mzalishaji akasema: "Unamaanisha nini kwa hili, kwamba umejipasulia msamba?" Basi akaitwa jina lake Perezi.[a] **30** Na baadaye ndugu yake ambaye mkono wake ulifungwa kitambaa chekundu akatoka naye jina lake akaitwa Zera.[b]

39 Basi Yosefu akapelekwa Misri,[c] na Potifa,[d] ofisa wa makao ya Farao, mkuu wa walinzi, Mmisri, akamnunua kutoka kwa Waishmaeli[e] waliokuwa wamemleta huko. **2** Lakini Yehova alikuwa pamoja na Yosefu hata akafanikiwa,[f] akaja kusimamia nyumba ya bwana wake, yule Mmisri. **3** Naye bwana wake akaona kwamba Yehova alikuwa pamoja naye na kwamba kila jambo alilokuwa akifanya Yehova alikuwa akilifanikisha mikononi mwake.

4 Na Yosefu akazidi kupata kibali machoni pake naye akamtumikia siku zote hata akamweka juu ya nyumba yake,[g] na vitu vyote vilivyokuwa vyake akaviweka mkononi mwake. **5** Ikawa kwamba tangu alipomweka asimamie nyumba yake na vyote vilivyokuwa vyake, Yehova akazidi kuibariki nyumba ya Mmisri huyo kwa sababu ya Yosefu, na Yehova akabariki vitu vyote alivyokuwa navyo nyumbani na shambani.[h] **6** Mwishowe akaweka katika mkono wa Yosefu vitu vyake vyote,[i] wala hakujua kilichokuwa chake ila mkate aliokuwa akila. Pia, Yosefu akakua akawa mwenye umbo zuri na mwenye sura ya kupendeza.

SURA 38
a Kum 23:17
b Met 6:33
Met 12:14
Met 18:3
Ro 6:21
2Ko 4:2
Efe 5:12
c Mwa 34:31
Hes 5:12
d Mwa 19:36
2Sa 11:5
e Law 21:9
Kum 24:16
f Mwa 38:16
Met 18:17
1Ko 4:5
g Mwa 31:32
Mwa 37:32
Law 19:15
h Mwa 38:18
i Ro 2:1
j 1Sa 24:17
Ayu 33:27
Met 11:6
k Mwa 38:11
Kum 25:5
Ru 3:12
l Ayu 34:32

Safu ya 2
a Mwa 46:12
Ru 4:12
1Nya 2:4
Lu 3:33
b 1Nya 9:6
Mt 1:3

SURA 39
c Zb 105:17
Mdo 7:9
d Mwa 37:36
e Mwa 17:20
Mwa 37:25
f Zb 1:3
Ro 8:31
Ebr 13:6
g Met 14:35
Lu 12:44
1Ko 4:2
h Mwa 30:27
Kum 28:3
2Sa 6:11
i Lu 16:10
Lu 19:17

7 Sasa baada ya mambo
hayo ikawa kwamba mke
wa bwana wake akaanza ku-
inua macho[a] yake kumwele-
kea Yosefu na kusema: "Lala
nami."[b] **8** Lakini akawa aki-
kataa,[c] naye alikuwa akimwa-
mbia mke wa bwana wake: "Ta-
zama bwana wangu hajui kili-
cho nami nyumbani, na vyote
ameviweka mkononi mwangu.[d]
9 Hakuna yeyote aliye mku-
bwa zaidi yangu katika nyu-
mba hii, naye hakunizuilia cho-
chote ila wewe, kwa sababu
wewe ni mke wake.[e] Basi ni-
nawezaje kufanya ubaya huu
mkubwa na kwa kweli nimte-
ndee Mungu dhambi?"[f]
10 Basi ikawa kwamba ali-
posema na Yosefu siku baada
ya siku, hakumsikiliza kamwe
alale kando yake, awe pamoja
naye.[g] **11** Lakini ikawa kwa-
mba siku hiyo sawa na siku
nyinginezo akaingia nyumba-
ni afanye kazi zake, na hapa-
kuwa na yeyote kati ya watu
wa nyumba aliyekuwa nda-
ni ya nyumba hiyo.[h] **12** Basi
mwanamke huyo akamshika
kwa vazi lake,[i] akisema:
"Lala nami!"[j] Lakini akalia-
cha vazi lake mkononi mwa-
ke, akakimbia na kwenda nje.[k]
13 Basi mara huyo mwanamke
alipoona ya kuwa ameliacha
vazi lake mkononi mwake ili
aweze kukimbia nje, **14** aka-
anza kuwaita watu wa nyu-
mba yake kwa sauti kubwa na
kuwaambia: "Tazameni! Alitu-
letea mtu, Mwebrania, atufa-
nyie dhihaka. Alinijia ili alale
nami, lakini nikalia kwa sauti
kubwa.[l] **15** Na mara tu alipo-
sikia nimepaaza sauti na kua-
nza kulia, akaliacha vazi lake
kando yangu, akakimbia nje."

SURA 39
a Mt 5:28
2Pe 2:14
b Law 20:10
Met 2:16
1Ko 6:9
c Met 1:10
Met 5:20
Met 22:6
d Lu 16:12
1Ko 4:2
e Met 6:29
Mk 10:8
f Mwa 2:24
Mwa 20:6
Zb 51:4
Ga 5:19
Ebr 13:4
g Met 5:3
Met 22:14
h Ayu 24:15
Yer 23:24
i Mhu 7:26
Yak 1:14
j 2Sa 13:11
k Met 6:32
1Ko 6:18
2Ti 2:22
l Zb 35:20
Met 6:19
Met 12:17

Safu ya 2
a Zb 37:12
b Kut 20:16
Met 12:22
Met 19:5
c Kum 19:15
Met 6:34
Met 29:12
d Zb 105:18
1Pe 2:20
1Pe 3:14
e Mwa 40:3
Zb 105:19
Met 16:7
Da 1:9
Mdo 7:9
f Mwa 39:6
g Mwa 49:22
Zb 1:3
Mdo 7:10

SURA 40
h Mwa 40:11
Mwa 41:9
i Mdo 7:10

16 Baada ya hayo akaliweka
vazi lake kando yake mpaka
bwana wake aliporudi nyumba-
ni kwake.[a]
17 Kisha akamwambia ma-
neno hayo, akisema: "Yule mtu-
mishi Mwebrania uliyetuletea
alinijia ili anidhihaki. **18** La-
kini mara tu nilipopaaza sau-
ti na kulia, akaliacha vazi lake
kando yangu, akakimbia nje."[b]
19 Ikatokea kwamba mara tu
bwana wake aliposikia maneno
ya mke wake, akisema: "Mtu-
mishi wako alinifanyia hivi na
hivi," hasira yake ikawaka.[c]
20 Basi bwana wa Yosefu aka-
mchukua akamtia katika nyu-
mba ya gereza, mahali ambapo
wafungwa wa mfalme waliwe-
kwa kizuizini, naye akaendelea
kuwa humo katika nyumba ya
gereza.[d]
21 Hata hivyo, Yehova aka-
endelea kuwa pamoja na Yo-
sefu, akazidi kumfanyia fadhi-
li zenye upendo na kumwezesha
kupata kibali machoni pa ofi-
sa mkuu wa nyumba ya gere-
za.[e] **22** Ofisa mkuu wa nyu-
mba ya gereza akawatia mkono-
ni mwa Yosefu wafungwa wote
waliokuwa katika nyumba hiyo
ya gereza; na yote waliyoku-
wa wakifanya humo yeye ndi-
ye aliyekuwa akiagiza yafa-
nywe.[f] **23** Yule ofisa mkuu wa
nyumba ya gereza hakuwa aki-
angalia kitu chochote kilicho-
kuwa mkononi mwake, kwa sa-
babu Yehova alikuwa pamoja na
Yosefu na yale aliyokuwa akifa-
nya Yehova aliyafanikisha.[g]

40 Sasa ikawa kwamba ba-
ada ya mambo hayo,
mnyweshaji[h] wa mfalme wa
Misri na mwokaji walimte-
ndea dhambi bwana wao,
mfalme wa Misri.[i] **2** Farao

akakasirishwa na hao watumishi wake wawili,[a] mkuu wa wanyweshaji na mkuu wa waokaji.[b] **3** Basi akawatia katika jela ya nyumba ya mkuu wa walinzi,[c] katika ile nyumba ya gereza,[d] mahali ambapo Yosefu alikuwa mfungwa. **4** Kisha mkuu wa walinzi akampa Yosefu mgawo awe nao ili awahudumie;[e] nao wakakaa jela siku kadhaa.

5 Na wote wawili wakaota ndoto,[f] kila mmoja ndoto yake katika huo usiku mmoja,[g] kila mmoja ndoto yake yenye tafsiri yake,[h] mnyweshaji na mwokaji wa mfalme wa Misri waliokuwa wafungwa katika nyumba ya gereza.[i] **6** Yosefu alipowajia asubuhi na kuwaona, tazama, walionekana wana huzuni.[j] **7** Naye akawauliza hao maofisa wa Farao waliokuwa naye katika jela ya nyumba ya bwana wake, akisema: "Kwa nini nyuso zenu zina huzuni leo?"[k] **8** Wakamjibu: "Tumeota ndoto, wala hatuna mtafsiri." Basi Yosefu akawaambia: "Je, tafsiri si za Mungu?[l] Tafadhali, nisimulieni."

9 Naye mkuu wa wanyweshaji akamsimulia Yosefu ndoto yake akisema: "Katika ndoto yangu, kulikuwako mzabibu mbele yangu. **10** Na kwenye mzabibu kulikuwako matawi matatu, na ulionekana unaota machipukizi.[m] Ukachanua maua. Vishada vyake vikaivisha zabibu zake. **11** Kikombe cha Farao kilikuwa mkononi mwangu, nami nikachukua zabibu na kuziminya ndani ya kikombe cha Farao.[n] Halafu nikakiweka kikombe mkononi mwa Farao."[o] **12** Kisha Yosefu akamwambia: "Hii ndiyo tafsiri yake.[a] Yale matawi matatu ni siku tatu. **13** Baada ya siku tatu Farao atakiinua kichwa chako naye atakurudisha katika cheo chako;[b] nawe bila shaka utampa Farao kikombe mkononi mwake, kulingana na desturi ya zamani ulipokuwa mnyweshaji wake.[c] **14** Hata hivyo, unikumbuke mara tu mambo yatakapokuendea vema,[d] tafadhali, usikose kunitendea fadhili zenye upendo na kunitaja kwa Farao,[e] nawe unitoe nje ya nyumba hii. **15** Kwa maana kwa kweli nilitekwa nyara kutoka katika nchi ya Waebrania;[f] na hapa pia sijafanya jambo lolote kamwe hata wanitie katika tundu hili la gereza."[g]

16 Mkuu wa waokaji alipoona kwamba Yosefu ametafsiri jambo jema, yeye naye akamwambia Yosefu: "Mimi pia nilikuwa katika ndoto yangu, na tazama, vikapu vitatu vya mkate mweupe vilikuwa kichwani pangu. **17** Ndani ya kikapu cha juu kabisa mlikuwemo namna zote za vyakula vya Farao,[h] vitu vya mwokaji, pia kulikuwako ndege[i] wakizila katika kikapu juu ya kichwa changu." **18** Kisha Yosefu akajibu na kusema: "Hii ndiyo tafsiri yake:[j] Vile vikapu vitatu ni siku tatu. **19** Baada ya siku tatu tokea sasa Farao atakiinua kichwa chako na kukiondoa juu yako naye atakutundika juu ya mti;[k] nao ndege wataila nyama yako."[l]

20 Basi siku ya tatu ilikuwa sikukuu ya kuzaliwa kwa Farao,[m] naye akawafanyia karamu watumishi wake wote na kukiinua kichwa cha mkuu wa wanyweshaji na kichwa

SURA 40

a Mwa 41:10
Met 16:14
Met 19:12
b Mwa 40:20
c Mwa 37:36
d Mwa 39:20
Zb 105:18
e Mwa 39:22
f Ayu 33:15
g Mwa 41:11
h Mwa 41:12
i Mwa 41:10
j Met 15:13
Da 1:10
k Lu 24:17
l Mwa 41:16
Zb 25:14
Da 2:28
Da 2:45
m Hes 13:23
n Met 3:10
o Mwa 40:21

Safu ya 2

a Mwa 41:12
Da 2:30
b Mwa 40:21
Mwa 41:13
Yer 52:31
c Ne 2:1
d 1Sa 25:31
Lu 23:42
e 2Sa 9:1
f Mwa 14:13
Mwa 37:28
Mwa 41:12
Kut 21:16
Mdo 7:9
g Mwa 39:8
Zb 105:19
Zb 119:86
Da 6:22
Yoh 15:25
Ebr 12:11
1Pe 3:17
h Mwa 49:20
1Nya 12:40
i Mwa 15:11
j Mwa 41:12
k Mwa 41:13
Kum 21:22
Yos 8:29
Yos 10:26
l 1Sa 17:44
2Sa 21:10
Yer 16:4
Eze 39:4
Ufu 19:17
m Mhu 7:1
Mk 6:21

cha mkuu wa waokaji katikati
ya watumishi wake.[a] **21** Aka-
mrudisha mkuu wa wanywe-
shaji kwenye cheo chake cha
kunywesha,[b] naye akaendelea
kumpa Farao kikombe mkono-
ni mwake. **22** Lakini aka-
mtundika mkuu wa waokaji,[c]
kama vile Yosefu alivyokuwa
amewatafsiria.[d] **23** Hata hi-
vyo, mkuu wa wanyweshaji
hakumkumbuka Yosefu, naye
akaendelea kumsahau.[e]

41 Ikawa kwamba mwisho-
ni mwa miaka miwili
kamili Farao akaota ndoto,[f]
na tazama, alikuwa amesi-
mama kando ya mto Nile.
2 Na tazama, ng'ombe saba,
wenye sura nzuri, wanono, wa-
katoka ndani ya mto Nile, nao
wakaanza kula majani ya mto
Nile.[g] **3** Na tazama, baada
yao ng'ombe wengine saba wa-
katoka ndani ya mto Nile, we-
nye sura mbaya, waliokonda,[h]
nao wakasimama kando ya
wale ng'ombe waliokuwa uki-
ngoni mwa mto Nile. **4** Kisha
wale ng'ombe waliokuwa na
sura mbaya, waliokonda, wa-
kaanza kuwala wale ng'ombe
saba waliokuwa na sura nzu-
ri, wanono.[i] Basi Farao aka-
amka.[j]
5 Hata hivyo, akarudi kula-
la usingizi na kuota ndoto mara
ya pili. Na tazama, kulikuwa na
masuke saba ya nafaka yakito-
keza kwenye tawi moja, maku-
bwa na mazuri.[k] **6** Na taza-
ma, kulikuwa na masuke saba
ya nafaka, membamba, yaliyo-
unguzwa na upepo wa masha-
riki,[l] yakikua baada ya yale
mengine.[m] **7** Nayo yale masu-
ke membamba ya nafaka ya-
kaanza kuyameza yale masuke
saba ya nafaka, makubwa, yali-

SURA 40
a Met 16:14
b Ne 2:1
c Mwa 41:13
Est 7:10
d Mwa 40:8
Da 2:30
e Mwa 40:14
Ayu 19:14

SURA 41
f Mwa 20:3
Mwa 40:5
Ayu 33:15
Da 2:1
g Mwa 1:30
Mwa 41:18
h Mwa 41:19
i Mwa 41:20
j Mwa 41:21
1Fa 3:15
k Mwa 41:22
l 2Fa 19:26
Eze 17:10
Ho 13:15
m Mwa 41:23

Safu ya 2
a Mwa 41:24
b Da 2:1
c Kut 7:11
d Isa 19:11
Da 2:2
1Ko 3:20
e Da 4:7
f Mwa 40:21
g Met 28:13
h Mwa 40:2
i Mwa 37:36
Mwa 40:3
j Mwa 40:5
k Mwa 39:17
l Mwa 39:1
m Mwa 40:8
n Mwa 40:21
o Mwa 40:22
p 1Sa 2:8
Zb 105:20
q Mwa 40:15
Da 2:25
r Yer 9:26
s Yer 52:33
t Zb 25:14
Da 5:12
Mdo 7:10

yojaa.[a] Basi Farao akaamka na
tazama ilikuwa ni ndoto tu.
8 Ikawa kwamba asubuhi,
roho yake ikafadhaika.[b] Basi
akawaita makuhani wote we-
nye kufanya uchawi wa Misri[c]
na watu wake wote wenye he-
kima,[d] naye Farao akawasimu-
lia ndoto zake.[e] Lakini hakuku-
wa na yeyote aliyeweza kumta-
fsiria Farao ndoto hizo.
9 Kisha mkuu wa wanywe-
shaji akaongea na Farao,[f] na
kusema: "Dhambi zangu ni-
nazitaja leo.[g] **10** Farao ali-
wakasirikia watumishi wake.[h]
Kwa hiyo akanitia katika jela
ya nyumba ya mkuu wa wali-
nzi,[i] mimi na mkuu wa waoka-
ji. **11** Kisha sote wawili tuka-
ota ndoto usiku mmoja, mimi
na yeye. Tuliota kila mmoja
ndoto yake yenye tafsiri yake.[j]
12 Na kijana mmoja alikuwa
humo pamoja nasi, Mwe-
brania,[k] mtumishi wa mkuu wa
walinzi.[l] Tulipomsimulia,[m] aka-
tutafsiria ndoto zetu. Aka-
mtafsiria kila mmoja kama ili-
vyokuwa ndoto yake. **13** Ika-
wa kwamba kama vile alivyotu-
tafsiria, ndivyo ilivyotukia.
Mimi akanirudisha katika cheo
changu,[n] lakini yeye akamtu-
ndika."[o]
14 Na Farao akatuma watu
wamwite Yosefu,[p] kwamba wa-
mlete upesi kutoka katika tu-
ndu la gereza.[q] Basi akajinyoa[r]
na kubadili nguo zake za kuji-
tanda,[s] akaingia ndani kwa
Farao. **15** Kisha Farao aka-
mwambia Yosefu: "Nimeo-
ta ndoto, lakini hapana mtu
wa kuitafsiri. Sasa mimi mwe-
nyewe nimesikia ikisemwa juu
yako ya kwamba unaweza kusi-
kia ndoto na kuitafsiri."[t]
16 Ndipo Yosefu akamjibu

Farao, akisema: "Mimi sipaswi
kufikiriwa! Mungu atamtanga-
zia Farao hali njema."[a]
17 Naye Farao akamwambia
Yosefu: "Katika ndoto yangu
tazama nilikuwa nimesima-
ma ukingoni mwa mto Nile.
18 Na tazama, ng'ombe saba
wanono, wenye umbo zuri wa-
katoka ndani ya mto Nile,
nao wakaanza kula majani ya
mto Nile.[b] **19** Na tazama,
ng'ombe wengine saba waka-
toka baada yao, dhaifu na we-
nye umbo baya sana, waliokon-
da.[c] Sijapata kuwaona waba-
ya kama hao katika nchi yote
ya Misri. **20** Na wale ng'o-
mbe waliokonda, wabaya,
wakaanza kuwala wale ng'o-
mbe saba wanono wa kwanza.[d]
21 Basi hao wakaingia matu-
mboni mwao, na bado hainge-
weza kujulikana kwamba wa-
likuwa wameingia matumboni
mwao, kwa kuwa sura zao zi-
likuwa mbaya kama vile mwa-
nzoni.[e] Ndipo nilipoamka.
22 "Kisha nikaona katika
ndoto yangu na tazama, ku-
likuwa na masuke saba ya na-
faka yakitokeza kwenye tawi
moja, yaliyojaa na mazuri.[f]
23 Na tazama, kulikuwa na
masuke saba ya nafaka ya-
liyokauka, membamba, yali-
younguzwa na upepo wa ma-
shariki,[g] yakikua baada yake.
24 Na yale masuke membamba
ya nafaka yakaanza kuyameza
yale masuke saba ya nafaka ya-
liyo mazuri.[h] Basi nikawasimu-
lia makuhani wenye kufanya
uchawi,[i] lakini hakuwako yeyo-
te aliyeniambia."[j]
25 Kisha Yosefu akamwa-
mbia Farao: "Ndoto ya Farao
ni moja. Anayofanya Mungu
wa kweli amemwambia Farao.[k]

SURA 41
a Mwa 40:8
Da 2:23
Da 2:28
b Mwa 41:2
c Mwa 41:3
d Mwa 41:4
e Law 26:26
Isa 9:20
f Mwa 41:5
g Mwa 41:6
Zb 129:6
h Mwa 41:7
i Mwa 41:8
Kut 7:11
Da 2:2
j Da 2:27
Da 4:7
k Zb 98:2
Isa 41:22
Da 2:28
Amo 3:7

Safu ya 2
a Kut 14:21
b Mwa 12:10
2Fa 8:1
c Da 2:28
d Isa 24:4
Mt 24:7
Mdo 7:11
Mdo 11:28
e Kum 19:15
Ayu 33:14
Mt 18:16
f 2Th 3:1
g Kum 1:13
1Ko 4:2
h 1Fa 11:28
i Mwa 41:47
Mwa 47:26
j Mwa 41:48
Met 8:21
Mdo 7:12

26 Wale ng'ombe saba wazuri
ni miaka saba. Hali kadhalika
yale masuke saba ya nafaka ya-
liyo mazuri ni miaka saba. Ndo-
to ni moja. **27** Nao wale ng'o-
mbe saba waliokonda ambao
walipanda baada yao ni miaka
saba; na yale masuke saba ya
nafaka yaliyo matupu, yaliyo-
unguzwa na upepo wa masha-
riki,[a] yatakuwa miaka saba
ya njaa.[b] **28** Hilo ndilo jambo
ambalo nimemwambia Farao:
Anayofanya Mungu wa kweli
amemwezesha Farao kuona.[c]
29 "Tazama kuna miaka
saba inayokuja ya shibe katika
nchi yote ya Misri. **30** Laki-
ni miaka saba ya njaa itakuja
baada yake, nayo shibe yote ya
nchi ya Misri itasahaulika nayo
njaa itaimaliza nchi.[d] **31** Na
shibe iliyokuwako wakati
mmoja katika nchi haitajulika-
na kwa sababu ya njaa itakayo-
fuata, kwa kuwa itakuwa kali
sana. **32** Na kwa kuwa ndoto
hiyo ilirudiwa mara mbili kwa
Farao inamaanisha kwamba ja-
mbo hilo limewekwa imara na
Mungu wa kweli,[e] na Mungu
wa kweli anaharakisha kulifa-
nya.[f]
33 "Basi sasa Farao na ata-
fute mtu mwenye busara na
mwenye hekima, amweke juu
ya nchi ya Misri.[g] **34** Farao
na achukue hatua na kuwa-
weka waangalizi juu ya nchi,[h]
naye achukue sehemu moja ya
tano ya nchi ya Misri waka-
ti wa ile miaka saba ya shi-
be.[i] **35** Nao wakusanye vya-
kula vyote vya miaka hiyo mi-
zuri inayokuja, nao warundi-
ke nafaka chini ya mkono wa
Farao zikiwa vyakula majijini,[j]
nao waviweke akiba. **36** Na-
vyo vyakula hivyo viwe akiba

ya nchi kwa ajili ya ile miaka
saba ya njaa, itakayotokea ka-
tika nchi ya Misri,[a] ili hii nchi
isije ikafutiliwa mbali na hiyo
njaa."[b]
37 Basi jambo hilo likawa
jema machoni pa Farao na wa-
tumishi wake wote.[c] **38** Kwa
hiyo Farao akawaambia watu-
mishi wake: "Je, kwaweza ku-
patikana mtu mwingine kama
huyu ambaye roho ya Mu-
ngu imo ndani yake?"[d] **39** Ki-
sha Farao akamwambia Yose-
fu: "Kwa kuwa Mungu ameku-
wezesha kuyajua yote hayo,[e]
hakuna mtu mwenye busara na
mwenye hekima kama wewe.[f]
40 Wewe binafsi utaisimamia
nyumba yangu,[g] na watu wa-
ngu wote watakutii kabisa.[h]
Mimi nitakuwa mkuu kuliko
wewe katika kiti cha ufalme
tu."[i] **41** Tena Farao akamwa-
mbia Yosefu: "Ona, nakuwe-
ka juu ya nchi yote ya Misri."[j]
42 Kisha Farao akaivua pete
yake rasmi ya muhuri[k] ku-
toka mkononi mwake, akai-
weka mkononi mwa Yosefu
na kumvalisha mavazi ya kita-
ni bora, naye akaweka mkufu
wa dhahabu shingoni mwake.[l]
43 Tena akampandisha katika
gari la pili la heshima alilokuwa
nalo,[m] hata wapaaze sauti
mbele yake, *"Avrekh!"* hivyo
akamweka juu ya kila kitu ka-
tika nchi ya Misri.
44 Tena Farao akamwambia
Yosefu: "Mimi ni Farao, laki-
ni bila ruhusa yako mtu yeyo-
te asiinue mkono wake wala
mguu wake katika nchi yote ya
Misri."[n] **45** Kisha Farao aka-
liita jina la Yosefu Zafenath-
panea, naye akampa Asenathi,[o]
binti ya Potifera kuhani wa
Oni,[p] awe mke wake. Naye Yo-
sefu akaanza kwenda kote-
kote katika nchi ya Misri.[a]
46 Naye Yosefu alikuwa na
umri wa miaka 30[b] aliposima-
ma mbele ya Farao mfalme wa
Misri.
Kisha Yosefu akatoka mbe-
le ya Farao, akatembea kote-
kote katika nchi yote ya Misri.
47 Na wakati wa ile miaka saba
ya shibe nchi ikaendelea kuzaa
kwa wingi.[c] **48** Naye akaku-
sanya vyakula vyote vya ile mi-
aka saba iliyoijia nchi ya Misri,
akaviweka vyakula hivyo ma-
jijini.[d] Vyakula vya shamba li-
lilolizunguka jiji akaviweka
katikati yake.[e] **49** Na Yose-
fu akaendelea kurundika nafa-
ka nyingi sana,[f] kama mchanga
wa baharini, mpaka mwishowe
wakaacha kuihesabu, kwa sa-
babu haikuwa na hesabu.[g]
50 Na kabla ya ule mwaka
wa njaa kufika, Yosefu aka-
zaa wana wawili,[h] ambao Ase-
nathi, binti ya Potifera kuhani
wa Oni, alimzalia. **51** Basi Yo-
sefu akamwita jina lake mza-
liwa wa kwanza Manase,[i] kwa
sababu, kama alivyosema, "Mu-
ngu amenifanya nisahau taa-
bu yangu yote na nyumba yote
ya baba yangu."[j] **52** Naye yule
wa pili akamwita jina lake Efra-
imu,[k] kwa sababu, kama alivyo-
sema, "Mungu ameniwezesha
kuwa na uzao katika nchi ya ta-
abu yangu."[l]
53 Mwishowe miaka saba ya
shibe katika nchi ya Misri ikai-
sha,[m] **54** nayo miaka saba ya
njaa ikaanza kuja, kama vile tu
Yosefu alivyokuwa amesema.[n]
Nayo njaa ikawa katika nchi
zote, lakini mkate ulipatika-
na katika nchi yote ya Misri.[o]
55 Mwishowe nchi yote ya Mi-
sri ikawa na njaa, nao watu

SURA 41
a Mwa 47:13
b Mwa 45:11
Mwa 47:19
c Da 1:20
d Hes 27:18
Ayu 32:8
Isa 61:1
Da 4:8
e Zb 32:8
Met 14:35
1Ko 1:27
f Met 2:6
1Ko 2:6
g Mwa 39:6
Zb 105:21
Mdo 7:10
h Mwa 49:10
i Est 10:3
Da 6:3
j Da 5:7
k Est 8:10
Da 6:17
l Est 8:2
Zb 75:7
Da 5:29
m 1Fa 1:38
Est 6:11
n Mwa 44:18
Mwa 45:8
Mdo 7:10
o Mwa 46:20
p Yer 43:13
Eze 30:17

Safu ya 2
a Zb 105:21
b Hes 4:3
2Sa 5:4
Lu 3:23
c Mwa 26:12
Zb 65:9
d Kut 1:11
e 1Fa 9:19
2Nya 32:28
f Zb 107:37
g Kum 28:11
Mal 3:10
h Mwa 48:5
i Mwa 50:23
Hes 1:35
Ufu 7:6
j Zb 30:11
Isa 65:16
Ufu 21:4
k Mwa 48:17
Hes 1:33
Kum 33:17
Yos 14:4
l Zb 105:18
Zb 107:41
Amo 6:6
Mdo 7:10
m Mwa 41:26
n Mwa 41:30
Mdo 7:11
o Mwa 45:11
Mwa 47:17

wakaanza kumlilia Farao awape mkate.[a] Kisha Farao akawaambia Wamisri wote: "Nendeni kwa Yosefu. Lolote atakalowaambia, fanyeni."[b] **56** Na hiyo njaa ikawa juu ya uso wote wa dunia.[c] Ndipo Yosefu akaanza kuyafungua maghala yote ya nafaka yaliyokuwa kati yao na kuwauzia Wamisri,[d] ile njaa ilipozidi kuibana nchi ya Misri. **57** Tena, watu wa dunia yote wakaja Misri ili wanunue kutoka kwa Yosefu, kwa sababu hiyo njaa ilikuwa imeibana dunia yote.[e]

42 Mwishowe Yakobo akaona kwamba kuna nafaka Misri.[f] Kisha akawauliza wanawe: "Kwa nini mnaendelea kutazamana?" **2** Tena akawaambia: "Tazama nimesikia kwamba kuna nafaka Misri.[g] Shukeni huko mkatununulie nafaka, tupate kuendelea kuishi ili tusife." **3** Basi ndugu[h] kumi za Yosefu wakashuka waende kununua nafaka Misri. **4** Lakini Yakobo hakumruhusu Benyamini,[i] ndugu ya Yosefu, aende pamoja na wale ndugu zake wengine, kwa sababu alisema: "Ili tukio lenye kufisha lisimpate."[j]

5 Kwa hiyo wana wa Israeli wakafuatana na wengine waliokuwa wakienda kununua, kwa sababu kulikuwa na njaa katika nchi ya Kanaani.[k] **6** Na Yosefu ndiye aliyekuwa mwenye mamlaka juu ya nchi hiyo.[l] Ndiye aliyewauzia watu wote wa dunia.[m] Basi ndugu za Yosefu wakaja na kumwinamia kifudifudi.[n] **7** Yosefu alipowaona ndugu zake, akawatambua mara moja, lakini akajifanya asitambulike kwao.[o] Basi, akaongea nao kwa ukali na kusema: "Mmetoka wapi?" nao wakajibu: "Tumetoka nchi ya Kanaani ili kununua vyakula."[a]

8 Hivyo Yosefu akawatambua ndugu zake, lakini wao hawakumtambua. **9** Papo hapo Yosefu akakumbuka ndoto alizokuwa ameota juu yao,[b] naye akaendelea kuwaambia: "Ninyi ni wapelelezi! Mmekuja kuona hali ya ukosefu wa ulinzi wa nchi hii!"[c] **10** Kisha wakamwambia: "Sivyo, bwana wangu,[d] bali watumishi wako[e] wamekuja kununua vyakula. **11** Sisi sote ni wana wa mtu mmoja tu. Sisi ni watu wanyoofu. Watumishi wako si wapelelezi."[f] **12** Lakini akawaambia: "Sivyo! Kwa sababu ninyi mmekuja kuona hali ya ukosefu wa ulinzi wa hii nchi!"[g] **13** Ndipo wakamwambia: "Watumishi wako ni ndugu kumi na wawili.[h] Sisi ni wana wa mtu mmoja[i] tu katika nchi ya Kanaani; na tazama, yule mdogo zaidi yuko na baba yetu leo,[j] naye yule mwingine hayuko."[k]

14 Hata hivyo, Yosefu akawaambia: "Ni kama nilivyowaambia, nikisema: 'Ninyi ni wapelelezi!' **15** Hivyo ndivyo mtakavyojaribiwa. Kama Farao anavyoishi, hamtatoka hapa mpaka ndugu yenu mdogo atakapokuja hapa.[l] **16** Mtumeni mmoja wenu akamlete ndugu yenu, huku ninyi mkiwa mmefungwa, ili maneno yenu yajaribiwe kama ni ya kweli.[m] Ikiwa sivyo, basi, kama Farao anavyoishi, ninyi ni wapelelezi." **17** Kisha akawatia pamoja kifungoni kwa siku tatu.

18 Baada ya hayo Yosefu akawaambia siku ya tatu. "Fa-

SURA 41
a Mwa 47:13
Omb 5:10
b Zb 105:21
Zb 146:7
c Mwa 43:1
Lu 4:25
d Mwa 41:48
Mwa 47:16
Met 11:26
e Mwa 47:4
Zb 33:19

SURA 42
f Mwa 41:48
g Mdo 7:12
h 1Nya 2:1
i Mwa 35:18
Mwa 42:38
Mwa 44:20
j Mwa 43:14
k Mwa 41:57
Mdo 7:11
l Mwa 41:44
Mwa 45:8
Zb 105:21
Mdo 7:10
m Mwa 47:14
n Mwa 37:7
Mwa 37:9
o Mwa 42:23
Zb 81:5

Safu ya 2
a Mwa 37:1
Mdo 7:12
b Mwa 37:7
Mwa 37:9
Hes 12:6
c Mwa 47:13
d Ro 13:7
e Mwa 37:8
f Mwa 42:31
g Mwa 41:30
h 1Nya 2:1
i Kut 1:1
j Mwa 35:18
Mwa 42:38
Mwa 43:7
k Mwa 37:27
Mwa 37:35
Mwa 44:20
Mwa 45:26
Mdo 7:9
l Mwa 42:34
Mwa 43:29
m Zb 7:9

nyeni hili ili mwendelee kuishi. Mimi ninamwogopa[a] Mungu wa kweli. **19** Ikiwa ninyi ni wanyoofu, acheni mmoja wa ndugu zenu afungwe katika nyumba yenu ya kifungo,[b] lakini ninyi wengine mwende, chukueni nafaka kwa sababu ya njaa iliyo katika nyumba zenu.[c] **20** Kisha mtaniletea ndugu yenu mdogo, ili maneno yenu yaonekane kuwa yenye kutegemeka; nanyi hamtakufa."[d] Basi wakafanya hivyo.

21 Nao wakaanza kusemezana: "Bila shaka tuna hatia kuhusiana na ndugu yetu,[e] kwa sababu tuliona nafsi yake ikitaabika alipotuomba kwa bidii tumwonee huruma, lakini sisi hatukusikiliza. Ndiyo sababu taabu hii imetupata."[f] **22** Kisha Rubeni akawajibu, akawaambia: "Je, sikuwaambia, 'Msimtendee mtoto huyo dhambi,' lakini hamkusikia?[g] Na sasa damu yake inadaiwa tena."[h] **23** Lakini wao hawakujua kwamba Yosefu alikuwa akisikiliza, kwa sababu kulikuwako mtafsiri kati yao. **24** Basi akajitenga nao, akaanza kulia.[i] Kisha akarudi kwao, akaongea nao, akamchukua Simeoni[j] kati yao na kumfunga mbele ya macho yao.[k] **25** Baada ya hayo Yosefu akatoa amri, nao wakavijaza kabisa vyombo vyao nafaka. Pia, walipaswa kurudisha pesa za watu hao kwenye gunia la kila mmoja wao[l] na kuwapa vyakula kwa ajili ya safari.[m] Ndivyo walivyofanyiwa.

26 Basi wakapakia nafaka yao juu ya punda zao na kuondoka huko. **27** Mmoja wao alipofungua gunia lake ili ampe punda wake chakula wakiwa mahali pa kukaa usiku,[a] akaona pesa zake, na tazama, zilikuwa katika kinywa cha mfuko wake.[b] **28** Basi akawaambia ndugu zake: "Pesa zangu zimerudishwa na tazama, ziko hapa mfukoni mwangu!" Ndipo mioyo yao ikazimia, hivi kwamba wakageukiana wakitetemeka,[c] wakisema: "Ni nini hili Mungu ametutendea?"[d]

29 Mwishowe wakafika kwa Yakobo baba yao katika nchi ya Kanaani, wakamwambia mambo yote yaliyokuwa yamewapata, wakisema: **30** "Bwana wa nchi hiyo alisema nasi kwa ukali,[e] kwa kuwa alituwazia kuwa sisi ni watu wanaoipeleleza nchi.[f] **31** Lakini tukamwambia, 'Sisi ni watu wanyoofu.[g] Sisi si wapelelezi. **32** Sisi ni ndugu kumi na wawili,[h] wana wa baba yetu.[i] Mmoja hayuko,[j] na yule mdogo leo yuko na baba yetu katika nchi ya Kanaani.'[k] **33** Lakini huyo mtu aliye bwana wa nchi hiyo akatuambia,[l] 'Kwa njia hii nitajua kama ninyi ni wanyoofu:[m] Mmoja wa ndugu zenu akae nami.[n] Kisha chukueni vitu fulani kwa sababu ya njaa iliyo katika nyumba zenu, mwende.[o] **34** Nanyi mkamlete ndugu yenu mdogo, ili nijue kwamba ninyi si wapelelezi bali ni watu wanyoofu. Nitawarudishia ndugu yenu, nanyi mnaweza kufanya biashara yenu nchini.'"[p]

35 Ikawa kwamba walipokuwa wakitoa vilivyokuwa ndani ya magunia yao tazama, kifurushi cha pesa cha kila mmoja wao kilikuwa katika gunia lake. Na wao na baba yao pia wakapata kuona vifurushi vyao vya pesa, nao

SURA 42

a Mwa 20:11
Law 25:43
Ne 5:15
Met 8:13
2Ko 7:1
b Mwa 42:24
c Mwa 43:2
Mwa 45:23
d Mwa 43:5
Mwa 44:23
e Mwa 37:18
Mwa 37:28
Mwa 50:17
Mdo 7:9
f Hes 32:23
Met 21:13
Mt 7:2
1Ti 5:24
g Mwa 37:21
Ro 2:15
h Mwa 9:5
Zb 9:12
Ufu 6:10
i Mwa 43:30
j Mwa 42:19
Mwa 49:5
k Mwa 43:23
Ayu 36:8
l Mwa 44:1
m Mwa 45:21
1Pe 3:9

Safu ya 2

a Mwa 43:21
Met 12:10
Yer 9:2
Yer 41:17
b Mwa 43:21
c Law 26:36
Lu 19:21
d Isa 45:7
Amo 3:6
Ebr 10:30
e Mwa 42:7
f Yos 2:1
Amu 1:23
2Sa 10:3
g Mwa 42:11
Met 11:6
Met 14:2
h Mwa 42:13
i Mdo 7:8
j Mwa 37:28
Mwa 37:35
k Mwa 35:18
Mwa 42:4
l Mwa 45:9
m Met 14:9
n Mwa 42:19
o Mwa 42:2
Omb 4:9
p Mwa 34:10
Mwa 42:20
Yak 4:13

wakaogopa. **36** Kisha Yakobo baba yao akawaambia:
"Mmefanya mimi nifiwe!^a Yosefu hayuko naye Simeoni hayuko,^b na Benyamini mtamchukua! Mambo yote hayo yamenijia mimi!" **37** Lakini Rubeni akamwambia baba yake: "Nisipomrudisha kwako uwaue wanangu wawili.^c Nipe yeye, nami ndimi nitakayemrudisha kwako."^d **38** Lakini, akasema: "Mwanangu hatashuka kwenda nanyi, kwa sababu ndugu yake amekufa naye amebaki peke yake.^e Tukio lenye kufisha likimpata katika njia mtakayoiendea, basi bila shaka mtazishusha mvi zangu kwa huzuni mpaka katika Kaburi."*^f

43 Nayo njaa ilikuwa kali katika nchi.^g **2** Ikawa mara tu walipokuwa wamemaliza kuila nafaka waliyokuwa wameleta kutoka Misri,^h baba yao akawaambia: "Rudini, mkatunununulie chakula kidogo."^i **3** Kisha Yuda akamwambia:^j "Yule mtu alituhakikishia waziwazi, akisema, 'Msiuone uso wangu tena isipokuwa ndugu yenu awe pamoja nanyi.'^k **4** Ikiwa utamruhusu ndugu yetu aende nasi,^l tuko tayari kwenda kukununulia chakula. **5** Lakini ikiwa hutamruhusu aende nasi, hatutaenda, kwa sababu yule mtu alituambia, 'Msiuone uso wangu tena isipokuwa ndugu yenu awe pamoja nanyi.'"^m **6** Naye Israeli akasema:^n "Kwa nini mmenidhuru kwa kumwambia mtu huyo ya kwamba mna ndugu mwingine?" **7** Kisha wakasema: "Mtu huyo aliuliza moja kwa moja kutuhusu na kuhusu jamaa zetu, akisema, 'Je, baba yenu angali hai?^a Je, mna ndugu mwingine?' nasi tukamwambia kupatana na mambo hayo.^b Tungewezaje kujua kwamba kwa hakika atasema, 'Shukeni na ndugu yenu'?"^c

8 Mwishowe Yuda akamwambia Israeli baba yake: "Mruhusu huyu mvulana aende nami,^d ili tupate kuondoka twende na ili tuendelee kuishi ili tusife,^e sisi na wewe na watoto wetu wadogo.^f **9** Mimi nitakuwa dhamana kwa ajili yake.^g Umdai mkononi mwangu.^h Nisipomrudisha kwako na kumweka mbele yako, basi nitakuwa nimekutendea dhambi ya kudumu. **10** Lakini ikiwa hatungalikawia, kufikia sasa tungalikuwa tumefika huko na kurudi mara mbili hizi."^i

11 Kisha Israeli baba yao akawaambia: "Ikiwa, basi, ndivyo ilivyo,^j fanyeni hivi: Chukueni mali bora zaidi ya nchi katika vyombo vyenu mkampelekee mtu huyo iwe zawadi:^k zeri kidogo,^l na asali kidogo,^m ubani mweusi na gome lenye utomvu,^n kungu na lozi.^o **12** Pia chukueni pesa mara mbili mkononi mwenu; na pesa zilizorudishwa katika vinywa vya mifuko yenu mzirudishe zikiwa mkononi mwenu.^p Huenda lilikuwa kosa.^q **13** Nanyi mchukueni ndugu yenu, mwondoke, mrudi kwa mtu huyo. **14** Na Mungu Mweza-Yote na awape huruma mbele ya mtu huyo,^r ili amwachilie yule ndugu yenu mwingine na Benyamini. Lakini ikiwa nitafiwa, kwa kweli nitafiwa!"^s

SURA 42
a Mwa 43:14
b Mwa 37:28
Mwa 37:35
Mwa 42:24
c Mwa 37:22
Mwa 46:9
d Mwa 43:9
Mwa 44:32
e Mwa 37:33
Mwa 44:20
f Mwa 37:35
Hes 16:30
1Fa 2:6
Zb 49:14
Zb 89:48
Mhu 9:10
Ho 13:14
Mdo 2:27
Ufu 20:13

SURA 43
g Mwa 41:30
Mdo 7:11
h Mwa 42:2
Mdo 7:12
i Kum 2:6
j Mwa 29:35
k Mwa 42:15
l Mwa 42:20
Mwa 42:36
m Mwa 42:15
Mwa 44:26
n Mwa 32:28

Safu ya 2
a Mwa 43:27
b Mwa 42:13
c Mwa 42:16
d Mwa 37:26
Mwa 42:38
e Mwa 42:2
Omb 4:9
f Mdo 7:14
g Mwa 44:32
Yoh 15:13
h Kut 21:23
1Fa 20:39
Ro 5:7
i 1Nya 5:2
j 2Fa 7:4
Mdo 21:14
k Mwa 32:20
Met 18:16
l Kut 25:6
Est 2:12
Yer 8:22
Yer 46:11
Eze 27:17
m 1Sa 14:25
Met 25:16
Mt 3:4
n Mwa 37:25
o Hes 17:8
p Mwa 42:25
Mwa 42:35
q Ro 13:8
2Ko 8:21
Ebr 13:18
r Ne 1:11
Lu 1:50
2Ko 5:10
s Mwa 27:45
Mwa 42:36

Mwa 42:38* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

15 Basi hao watu wakachukua zawadi hiyo, nao wakachukua pesa mara mbili mkononi mwao na Benyamini. Kisha wakaondoka na kwenda zao Misri, wakasimama mbele ya Yosefu.[a] **16** Yosefu alipomwona Benyamini akiwa pamoja nao, akamwambia mara moja mtu aliyekuwa juu ya nyumba yake: "Wapeleke watu hawa nyumbani, uchinje wanyama na kufanya matayarisho,[b] kwa sababu watu hawa watakula pamoja nami mchana." **17** Bila kukawia yule mtu akafanya kama vile Yosefu alivyokuwa amesema.[c] Basi akawapeleka hao watu nyumbani kwa Yosefu. **18** Lakini hao watu wakaogopa kwa sababu walikuwa wamepelekwa nyumbani kwa Yosefu,[d] wakaanza kusema: "Tunaletwa hapa ili watuangukie na kutushambulia na kutuchukua tuwe watumwa na pia punda zetu kwa sababu ya pesa tulizorudi nazo katika mifuko yetu pale mwanzoni!"[e]

19 Kwa hiyo wakamkaribia yule mtu aliyekuwa juu ya nyumba ya Yosefu, wakaongea naye kwenye mwingilio wa nyumba hiyo, **20** nao wakasema: "Tunakuomba radhi, bwana wangu! Kwa kweli mwanzoni tulikuja kununua chakula.[f] **21** Lakini ikatukia kwamba tulipofika mahali pa kulala[g] na kuanza kufungua mifuko yetu, kumbe, pesa za kila mmoja wetu zilikuwa katika kinywa cha mfuko wake, pesa zetu zikiwa na uzani wake kamili. Kwa hiyo tungependa kuzirudisha kwa mikono yetu wenyewe.[h] **22** Nasi tumeleta pesa zaidi mikononi mwetu ili kununua chakula. Kwa hakika hatujui ni nani aliyeziweka pesa zetu mifukoni mwetu."[a] **23** Kisha akasema: "Mambo ni sawa kwenu. Msiogope.[b] Mungu wenu na Mungu wa baba yenu aliwapa hazina mifukoni mwenu.[c] Pesa zenu zilinifikia kwanza." Kisha akamleta Simeoni kwao.[d]

24 Basi yule mtu akawaleta nyumbani kwa Yosefu, akawapa maji wapate kuoshwa miguu yao,[e] naye akawapa chakula kwa ajili ya punda zao.[f] **25** Nao wakaitayarisha zawadi[g] kwa ajili ya Yosefu atakapokuja mchana, kwa sababu walikuwa wamesikia kwamba hapo ndipo wangekula mkate.[h] **26** Yosefu alipoingia nyumbani, wakampelekea zawadi iliyokuwa mkononi mwao ndani ya nyumba, wakajilaza chini kifudifudi mbele yake.[i] **27** Kisha akawauliza hali yao na kusema:[j] "Je, baba yenu, yule mzee mliyesema juu yake, anaendelea vema? Je, angali hai?"[k] **28** Wakajibu, wakasema: "Mtumishi wako baba yetu anaendelea vema. Angali hai." Kisha wakainama na kulala kifudifudi.[l]

29 Alipoinua macho yake na kumwona Benyamini ndugu yake, mwana wa mama yake,[m] akasema: "Je, huyu ni ndugu yenu, yule mdogo zaidi mliyeniambia juu yake?"[n] Naye akaongeza kusema: "Mungu na akuonyeshe kibali chake,[o] mwanangu." **30** Sasa Yosefu alikuwa akiharakisha, kwa sababu hisia zake za ndani zilianza kusisimuka kumwelekea ndugu yake,[p] hata akatafuta mahali pa kulilia, naye akaingia katika chumba cha ndani, akaanza kulia machozi humo.[q]

SURA 43

a Mwa 37:7
b Mwa 18:7
Met 9:2
c Mwa 41:40
d Mwa 20:11
Mwa 42:21
e Mwa 42:25
Mwa 42:35
f Mwa 42:3
g Mwa 42:27
Lu 2:7
h Kum 22:2
Mdo 20:33
Ro 13:8
Ebr 13:5
1Pe 2:12

Safu ya 2

a Mwa 43:12
b Amu 6:23
c Mhu 5:19
Mdo 17:25
d Mwa 42:24
e Mwa 18:4
Mwa 19:2
1Sa 25:41
Yoh 13:12
f Mwa 24:32
Amu 19:21
g Mwa 43:11
Met 18:16
h Mwa 43:16
Kut 2:20
Ayu 42:11
i Mwa 37:7
Mwa 42:6
j Kut 18:7
1Sa 17:22
k Mwa 43:7
l Mwa 37:9
2Sa 1:2
2Nya 24:17
m Mwa 35:24
n Mwa 42:13
o Hes 6:25
p 1Fa 3:26
Flp 1:8
Kol 3:12
q Mwa 42:24

31 Kisha akanawa uso wake, akatoka, akajizuia, akasema:[a] "Leteni chakula."[b] **32** Nao wakamletea chakula chake kando na kile chao kando na cha Wamisri waliokuwa wakila naye kando; kwa maana Wamisri hawangeweza kula chakula pamoja na Waebrania, kwa sababu hilo ni chukizo kwa Wamisri.[c]

33 Nao walikuwa wameketi mbele yake, mzaliwa wa kwanza kupatana na haki ya mzaliwa wa kwanza[d] naye yule mdogo zaidi kupatana na uchanga wake; na hao watu wakawa wakitazamana kwa mshangao. **34** Naye akawa akituma watu wachukue visehemu vya chakula kutoka mbele yake na kuwapelekea, lakini akawa akiongeza kisehemu cha Benyamini mara tano kuliko visehemu vya wale wengine wote.[e] Basi wakaendelea kula karamu na kunywa naye mpaka waliposhiba.[f]

44 Baadaye akamwamuru mtu aliyekuwa akisimamia nyumba yake,[g] akisema: "Ijaze mifuko ya watu hawa kwa chakula kwa kadiri wanavyoweza kuchukua. Utie pesa za kila mmoja wao katika kinywa cha mfuko wake.[h] **2** Lakini kiweke kikombe changu, kile kikombe cha fedha, katika kinywa cha mfuko wa yule mdogo zaidi pamoja na pesa za nafaka yake." Basi akafanya kupatana na neno la Yosefu alilokuwa amesema.[i]

3 Asubuhi kulikuwa kumepambazuka watu hao waliporuhusiwa kuondoka,[j] pamoja na punda zao. **4** Wakatoka nje ya jiji. Hawakuwa wameenda mbali wakati Yosefu alipomwambia mtu aliyekuwa akisimamia nyumba yake: "Ondoka! Wafuatilie watu hao nawe uhakikishe umewafikia na kuwaambia, 'Kwa nini mmelipa ubaya kwa wema?[a] **5** Je, kikombe hiki sicho anachonywea bwana wangu na ambacho hutumia kusoma ishara za bahati kwa ustadi?[b] Mmefanya kitendo kibaya.'"

6 Mwishowe akawafikia na kuwaambia maneno hayo. **7** Lakini wakamwambia: "Kwa nini bwana wangu anasema maneno kama hayo? Ni jambo lisilowaziwa kwamba watumishi wako wafanye lolote kama hilo. **8** Kwani, pesa tulizopata vinywani mwa mifuko yetu tulikurudishia kutoka nchi ya Kanaani.[c] Basi, tungewezaje kuiba fedha au dhahabu katika nyumba ya bwana wako?[d] **9** Mtumwa wako atakayepatikana nacho na afe, nasi tuwe watumwa kwa bwana wangu."[e] **10** Ndipo akasema: "Basi sasa na iwe hivyo kama mlivyosema.[f] Yule ambaye atapatikana kuwa nacho atakuwa mtumwa wangu,[g] lakini ninyi mtakuwa hamna hatia." **11** Kisha wakashusha chini upesi kila mmoja mfuko wake nao wakafungua kila mtu mfuko wake. **12** Naye akatafuta kwa uangalifu. Akaanzia kwa yule mkubwa zaidi na kumalizia kwa yule mdogo zaidi. Mwishowe kikombe kikapatikana katika mfuko wa Benyamini.[h]

13 Kisha wakararua nguo zao za kujitanda,[i] na kila mmoja akainua mzigo wake na kuurudisha juu ya punda wake, wakarudi jijini. **14** Naye Yuda[j] na ndugu zake wakaenda mpaka nyumbani kwa Yosefu, naye

SURA 43
a Mwa 45:1
b Mwa 43:25
c Mwa 46:34 Kut 8:26
d Mwa 49:3 Kum 21:17
e Mwa 45:22 Mt 20:15
f Amu 14:10 Ayu 1:4

SURA 44
g Mwa 43:16
h Mwa 42:25
i Mwa 41:40
j Mwa 19:2 Amu 19:5

Safu ya 2
a Zb 109:5 Met 17:13
b Mwa 44:15 Law 19:26
c Mwa 43:12
d Law 19:11 Met 29:24 1Pe 3:16
e Mdo 25:11
f Met 6:2
g Kut 22:3 Mt 18:25
h Mwa 44:2
i Mwa 37:29 Yos 7:6 Mdo 14:14
j Mwa 43:8 Mwa 44:32

bado alikuwamo; nao wakaanguka chini mbele yake.[a]
15 Yosefu akawaambia: "Ni tendo gani hili mlilolifanya? Je, hamkujua kwamba mimi naweza kusoma ishara za bahati kwa ustadi?"[b] **16** Yuda akajibu, akasema: "Tumwambie nini bwana wangu? Tuseme nini? Nasi tunaweza kuonyeshaje kuwa sisi ni waadilifu?[c] Mungu wa kweli amegundua kosa la watumwa wako.[d] Tazama sisi ni watumwa wa bwana wangu,[e] sisi na yule ambaye mkononi mwake kikombe kilipatikana!"
17 Lakini yeye akasema: "Ni jambo lisilowaziwa upande wangu kufanya hivyo![f] Mtu ambaye mkononi mwake kikombe hicho kilipatikana ndiye atakayekuwa mtumwa wangu.[g] Ninyi wengine, nendeni kwa amani kwa baba yenu."[h]

18 Sasa Yuda akamkaribia, akamwambia: "Nakuomba, bwana wangu, tafadhali mruhusu mtumwa wako aongee neno masikioni mwa bwana wangu,[i] wala usiache hasira[j] yako iwake juu ya mtumwa wako, kwa sababu wewe ni kama Farao.[k] **19** Bwana wangu aliwauliza watumwa wake, akisema, 'Je, mna baba au ndugu?' **20** Basi tukamwambia bwana wangu, 'Tuna baba aliye mzee na mtoto wa uzee wake, aliye mdogo zaidi.[l] Lakini ndugu yake amekufa hivi kwamba yeye tu ndiye aliyesalia wa mama yake,[m] na baba yake anampenda.' **21** Kisha ukawaambia watumwa wako, 'Mleteni kwangu nipate kumwona.'[n] **22** Lakini tukamwambia bwana wangu, 'Mvulana huyo hawezi kumwacha baba yake. Akimwacha, bila shaka baba yake atakufa.'[a]
23 Halafu ukawaambia watumwa wako, 'Ndugu yenu mdogo asiposhuka pamoja nanyi, msiuone uso wangu tena kamwe.'[b]

24 "Basi tukaenda kwa mtumwa wako, baba yangu, tukamwambia maneno ya bwana wangu. **25** Baadaye baba yetu akasema, 'Rudini, mkatununulie chakula kidogo.'[c]
26 Lakini tukamwambia, 'Hatuwezi kwenda. Ikiwa ndugu yetu mdogo yuko pamoja nasi tutaenda, kwa sababu hatuwezi kuuona uso wa mtu huyo ikiwa ndugu yetu mdogo hayuko pamoja nasi.'[d] **27** Kisha mtumwa wako, baba yangu, akatuambia, 'Ninyi wenyewe mnajua vizuri kwamba mke wangu alinizalia wana wawili tu.[e] **28** Baadaye mmoja aliniacha nami nikasema: "Ah, haikosi ameraruliwa vipande-vipande!"[f] nami sijamwona mpaka leo hii. **29** Mkimchukua huyu naye toka machoni pangu na apatwe na tukio lenye kufisha, bila shaka mtazishusha mvi zangu kwa msiba mpaka katika Kaburi.'*[g]

30 "Sasa basi, nikifika tu kwa mtumwa wako, baba yangu, bila mvulana huyu, na hali nafsi yake imeshikamana na nafsi ya mvulana huyu,[h]
31 basi bila shaka itatukia kwamba mara atakapoona kwamba huyu mvulana hayupo atakufa tu, na watumwa wako kwa kweli watazishusha mvi za mtumwa wako baba yetu kwa huzuni mpaka katika Kaburi.* **32** Kwa maana

SURA 44

a Mwa 37:7
Mwa 50:18
b Mwa 44:5
c Mt 7:20
d Mwa 37:28
Mwa 42:21
Met 28:17
Mdo 2:37
e Mwa 50:18
f Mwa 42:18
g Mwa 44:9
h Mwa 26:29
i Mwa 18:30
j Met 14:29
Met 19:11
Met 29:8
k Mwa 41:44
Mwa 45:8
l Mwa 42:13
Mwa 43:7
m Mwa 35:18
Mwa 37:33
n Mwa 42:15
Mwa 43:29

Safu ya 2

a Mwa 42:38
b Mwa 42:20
Mwa 43:3
c Mwa 43:2
d Mwa 43:5
e Mwa 29:18
Mwa 30:23
Mwa 35:18
Mwa 46:19
f Mwa 37:33
g Mwa 37:35
Mwa 42:38
Zb 16:10
Zb 88:3
Mhu 9:10
Ho 13:14
Mt 11:23
Mdo 2:31
Ufu 20:13
h 1Sa 18:1
2Sa 18:33

Mwa 44:29,* 31* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

mtumwa wako alijitoa kuwa
dhamana[a] ya mvulana huyu awa-
po mbali na baba yake, akisema,
'Nisipomrudisha kwako, basi ni-
takuwa nimemtendea baba ya-
ngu dhambi milele.'[b] **33** Tafa-
dhali sasa, basi, mtumwa wako
na abaki akiwa mtumwa badala
ya huyu mvulana ili apate kwe-
nda na ndugu zake.[c] **34** Kwa
maana ninawezaje kwenda kwa
baba yangu bila yeye nisije ni-
kautazama msiba utakaompata
baba yangu?"[d]

45 Hapo Yosefu hakuwe-
za kujizuia tena mbe-
le ya wote waliokuwa wamesi-
mama karibu naye.[e] Basi aka-
paaza sauti: "Mwondoeni kila
mtu kutoka kwangu!" Wala ha-
kuna mtu mwingine yeyote ali-
yesimama pamoja naye alipoji-
tambulisha kwa ndugu zake.[f]
2 Naye akaanza kupaaza
sauti yake akilia,[g] hivi kwa-
mba Wamisri wakaisikia na
nyumba ya Farao ikaisikia.
3 Mwishowe Yosefu akawaam-
bia ndugu zake: "Mimi ni Yo-
sefu. Je, baba yangu angali
hai?" Lakini ndugu zake hawa-
kuweza kumjibu kamwe, kwa
sababu waliingiwa na wasiwasi
kwa sababu yake.[h] **4** Basi Yo-
sefu akawaambia ndugu zake:
"Tafadhali, nikaribieni." Basi
wakamkaribia.

Kisha akawaambia: "Mimi ni
Yosefu ndugu yenu, mliyemuu-
za Misri.[i] **5** Lakini sasa msi-
huzunike[j] wala msijikasirikie
kwa sababu mliniuza huku;
kwa sababu Mungu alinituma
mbele yenu ili kuhifadhi uhai.[k]
6 Kwa maana huu ni mwa-
ka wa pili wa njaa duniani,[l]
na bado kuna miaka mitano
ambayo hakutakuwa na waka-
ti wa kulima wala mavuno.[m]

SURA 44
a Ro 16:4
b Mwa 43:9
1Fa 20:39
c Ro 9:3
d Est 8:6

SURA 45
e Mwa 43:30
f Mdo 7:13
g Ru 1:9
h Mk 6:50
i Mwa 37:28
Mdo 7:9
j 2Ko 2:7
k Mwa 47:25
Mwa 50:20
1Sa 2:6
Zb 33:19
Zb 105:17
l Mwa 41:30
Mwa 47:18
m 1Ko 9:10

Safu ya 2
a Mwa 46:26
b Ro 8:28
c Amu 17:10
Ayu 29:16
Zb 105:21
d Mwa 45:26
Mdo 7:10
1Yo 4:14
e Mwa 46:34
Mwa 47:1
Kut 8:22
Kut 9:26
f Mwa 47:12
Met 3:27
Mdo 7:14
g Mwa 42:23
h Mwa 33:4
Mwa 46:29
i Kut 4:27
1Sa 20:41
Lu 15:20

7 Kwa sababu hiyo Mungu ali-
nituma mbele yenu ili niwa-
wekee ninyi mabaki[a] duniani
na kuwaweka hai kwa woko-
vu mkubwa. **8** Basi sasa si ni-
nyi ambao mlinileta hapa,[b] ila
ni Mungu wa kweli, ili aniwe-
ke niwe baba[c] kwa Farao na
bwana kwa nyumba yake yote
na kuwa mtawala katika nchi
yote ya Misri.

9 "Nendeni upesi kwa baba
yangu, mkamwambie, 'Hivi
ndivyo mwana wako Yosefu
amesema: "Mungu ameniwe-
ka kuwa bwana wa nchi yote
ya Misri.[d] Njoo kwangu. Usika-
wie. **10** Ukae katika nchi ya
Gosheni,[e] uishi karibu nami,
wewe na wana wako na wana
wa wana wako na makundi
yako na mifugo yako na kila
kitu ulicho nacho. **11** Nami
nitakupa chakula huko, kwa
maana bado kuna miaka mita-
no ya njaa;[f] usije kuwa maskini
wewe na nyumba yako na kila
kitu ulicho nacho.'" **12** Na
tazama, macho yenu na macho
ya ndugu yangu Benyamini ya-
naona ya kwamba ni kinywa
changu kinachosema nanyi.[g]
13 Basi msikose kumwambia
baba yangu juu ya utukufu wa-
ngu wote katika Misri na kila
kitu ambacho mmeona; nanyi
mfanye haraka kumleta baba
yangu hapa."

14 Kisha akamwangukia
Benyamini shingoni na kuan-
za kulia, naye Benyami-
ni akalia shingoni pake.[h]
15 Akawabusu ndugu zake
wote akawalilia,[i] kisha ndugu
zake wakaongea naye.

16 Habari hizo zikasikiwa
nyumbani kwa Farao, ikisemek-
ana: "Ndugu za Yosefu wa-
mekuja!" Ikawa vema machoni

pa Farao na watumishi wake.[a]
17 Basi Farao akamwambia
Yosefu: “Waambie ndugu zako,
‘Fanyeni hivi: Wapakieni wa-
nyama wenu wa kubeba mi-
zigo mwingie nchi ya Kana-
ani,[b] **18** mchukue baba yenu
na watu wa nyumba zenu mje
hapa kwangu, niwape mema ya
nchi ya Misri; na mle unono
wa nchi.[c] **19** Na wewe mwe-
nyewe unaamriwa:[d] “Fanyeni
hivi: Jichukulieni magari ya
kukokotwa[e] kutoka nchi ya
Misri kwa ajili ya watoto wenu
na wake zenu, mkamchukue
baba yenu katika gari moja
mje hapa.[f] **20** Na jicho lenu li-
sihuzunikie vifaa vyenu,[g] kwa
sababu wema wa nchi yote ya
Misri ni wenu.’”’”[h]
21 Kisha wana wa Israeli
wakafanya hivyo, naye Yosefu
akawapa magari kama Farao
alivyoamuru, pia akawapa vya-
kula[i] vya njiani. **22** Akampa
kila mmoja wao nguo moja ya
kujitanda ya kubadili,[j] laki-
ni akampa Benyamini vipande
mia tatu vya fedha na nguo
tano za kujitanda za kubadi-
li.[k] **23** Na akampelekea baba
yake vitu hivi: punda kumi wa-
liochukua vitu vyema vya Mi-
sri na punda-jike kumi walio-
chukua nafaka na mkate na ri-
ziki kwa ajili ya baba yake njia-
ni. **24** Basi akawaaga ndugu
zake, nao wakaenda. Hata hi-
vyo, akawaambia: “Msigomba-
ne njiani.”[l]
25 Nao wakaanza kutoka
Misri na mwishowe wakaingia
nchi ya Kanaani kwa Yako-
bo baba yao. **26** Kisha waka-
mpasha habari, wakimwambia:
“Yosefu angali hai, naye ndiye
anayetawala nchi yote ya Mi-
sri!”[m] Lakini moyo wake uka-
fa ganzi, kwa sababu haku-
waamini.[a] **27** Walipoende-
lea kumwambia maneno yote
ya Yosefu aliyokuwa amewaa-
mbia na alipoona magari
ambayo Yosefu alikuwa ame-
tuma yamchukue, roho ya Ya-
kobo baba yao ikaanza kufufu-
ka.[b] **28** Kisha Israeli akasema:
“Inatosha! Yosefu mwanangu
angali hai! Ah, acha niende
nikamwone kabla sijafa!”[c]

46 Basi Israeli na wote
waliokuwa wake waka-
ondoka, wakafika Beer-she-
ba[d] naye akamtolea dhabihu
Mungu wa baba yake Isaka.[e]
2 Kisha Mungu akaongea na
Israeli katika maono ya usiku,
na kumwambia:[f] “Yakobo, Ya-
kobo!” naye akajibu, akasema:
“Mimi hapa!”[g] **3** Naye akae-
ndelea kusema: “Mimi ndiye
Mungu wa kweli,[h] Mungu wa
baba yako.[i] Usiogope kwenda
Misri, kwa maana nitakufa-
nya uwe taifa kubwa huko.[j]
4 Mimi mwenyewe nitashu-
ka pamoja nawe Misri nami ni-
takupandisha pia;[k] na Yosefu
ataweka mkono wake juu ya
macho yako.”[l]
5 Kisha Yakobo akaondoka
Beer-sheba, nao wana wa Isra-
eli wakaendelea kumsafirisha
Yakobo baba yao na watoto
wao na wake zao katika maga-
ri ambayo Farao alikuwa ame-
tuma yamsafirishe.[m] **6** Tena,
wakachukua mifugo yao na
mali zao, walizokuwa wameku-
sanya katika nchi ya Kanaani.[n]
Mwishowe wakafika Misri, Ya-
kobo na uzao wake wote pamo-
ja naye. **7** Aliwaleta wanawe
na wana wa wanawe pamoja
naye, binti zake na binti za wa-
nawe, naam, uzao wake wote,

SURA 45
a 2Sa 3:36
Est 1:21
b Mwa 42:25
Mwa 43:18
c Mwa 27:28
Mwa 47:6
d Mwa 41:40
e Mwa 45:27
Mwa 46:5
Hes 7:3
1Sa 6:14
f Mwa 47:9
g Mwa 46:6
h Isa 1:19
i Mwa 21:14
Mwa 42:25
j 2Fa 5:5
k Mwa 43:34
l Mwa 42:21
Zb 133:1
m Zb 105:21

Safu ya 2
a Mwa 42:38
Mwa 44:28
Lu 24:11
b Isa 57:15
1Ko 16:18
2Ko 7:13
c Mwa 46:30
Lu 2:29

SURA 46
d Mwa 21:31
e Mwa 31:42
Kut 3:6
Lu 20:37
f Hes 12:6
Ayu 33:15
g 1Sa 3:4
h Mwa 5:22
1Fa 18:21
1Ko 8:6
i Mwa 28:13
Mt 22:32
j Mwa 12:2
Kut 1:7
Kum 26:5
Zb 105:12
Mdo 7:17
k Mwa 15:16
Mwa 28:15
Mwa 47:29
Mwa 50:13
Kut 3:8
Zb 105:37
l Mwa 50:1
m Mwa 45:19
n Mwa 31:18
Mwa 36:7

pamoja naye, wakaingia Misri.[a]

8 Sasa haya ndiyo majina ya wana wa Israeli waliokuja Misri:[b] Yakobo na wanawe: mzaliwa wa kwanza wa Yakobo alikuwa Rubeni.[c]

9 Na wana wa Rubeni walikuwa Hanoki na Palu na Hezroni na Karmi.[d]

10 Na wana wa Simeoni[e] walikuwa Yemueli na Yamini na Ohadi na Yakini[f] na Zohari na Shauli[g] mwana wa mwanamke Mkanaani.

11 Na wana wa Lawi[h] walikuwa Gershoni,[i] Kohathi[j] na Merari.[k]

12 Na wana wa Yuda[l] walikuwa Eri[m] na Onani[n] na Shela[o] na Perezi[p] na Zera.[q] Lakini Eri na Onani walikufa katika nchi ya Kanaani.[r]

Na wana wa Perezi wakawa ni Hezroni[s] na Hamuli.[t]

13 Na wana wa Isakari[u] walikuwa Tola[v] na Puva[w] na Iobu na Shimroni.[x]

14 Na wana wa Zabuloni[y] walikuwa Seredi na Eloni na Yahleeli.[z]

15 Hawa ndio wana wa Lea,[a] aliomzalia Yakobo huko Padanaramu, na binti yake Dina.[b] Nafsi zote za wanawe na za binti zake zilikuwa ni 33.

16 Na wana wa Gadi[c] walikuwa Zifioni na Hagi na Shuni na Esboni, Eri na Arodi na Areli.[d]

17 Na wana wa Asheri[e] walikuwa Imna na Ishva na Ishvi na Beria,[f] na Sera dada yao.

Na wana wa Beria walikuwa Heberi na Malkieli.[g]

18 Hao ndio wana wa Zilpa,[h] ambaye Labani alimpa binti yake Lea. Mwishowe akamzalia Yakobo hao: nafsi 16.

SURA 46

a Hes 20:15
Zb 105:23
Isa 52:4
Mdo 7:15
b Kut 1:1
c Mwa 35:23
Mwa 49:3
1Nya 5:1
d Kut 6:14
Hes 26:5
e Mwa 29:33
f Hes 26:12
g Kut 6:15
1Nya 4:24
h Mwa 29:34
1Nya 6:16
i Kut 6:16
Hes 3:23
j Kut 6:18
Hes 3:27
1Nya 9:32
k Hes 3:33
1Nya 6:63
l Mwa 29:35
Mwa 49:10
Ufu 5:5
m Mwa 38:3
n Mwa 38:4
o Mwa 38:5
p Ru 4:12
Lu 3:33
q Mwa 38:30
r Mwa 38:7
Mwa 38:10
s Hes 26:21
t 1Nya 2:5
u Mwa 49:14
Yos 19:17
v Hes 26:23
w 1Nya 7:1
x Hes 26:24
y Mwa 30:20
Mwa 49:13
z Hes 26:26
a Mwa 35:23
b Mwa 30:21
c Mwa 30:11
Mwa 49:19
d Hes 26:15
e Mwa 30:13
Mwa 49:20
Kum 33:24
f Hes 26:44
g Hes 26:45
h Mwa 29:24
Mwa 35:26

Safu ya 2

a Mwa 29:18
Mwa 35:24
b Mwa 30:24
Mwa 49:22
c Mwa 35:18
Mwa 49:27
d Mwa 41:51
Mwa 48:14
e Mwa 41:52
f Mwa 41:50
g Hes 26:38
h 1Nya 7:6
i 1Nya 8:3
j Hes 26:40
k Hes 26:39
l 1Nya 7:12
m Mwa 30:6
Mwa 49:16
n Hes 26:42
o Mwa 30:8
Mwa 49:21
p Hes 26:48
q Hes 26:49
r Mwa 29:29
Mwa 35:25
s Mwa 35:11

19 Wana wa Raheli,[a] mke wa Yakobo, walikuwa Yosefu[b] na Benyamini.[c]

20 Na katika nchi ya Misri Yosefu alizaa, Manase[d] na Efraimu,[e] ambao Asenathi[f] binti ya Potifera kuhani wa Oni alimzalia.

21 Na wana wa Benyamini walikuwa Bela[g] na Bekeri[h] na Ashbeli, Gera[i] na Naamani,[j] Ehi na Roshi, Mupimu[k] na Hupimu[l] na Ardi.

22 Hao ndio wana wa Raheli ambao alimzalia Yakobo. Nafsi zote zilikuwa 14.

23 Na wana wa Dani[m] walikuwa Hushimu.[n]

24 Na wana wa Naftali[o] walikuwa Yahzeeli na Guni[p] na Yezeri na Shilemu.[q]

25 Hao ndio wana wa Bilha,[r] ambaye Labani alimpa Raheli binti yake. Mwishowe akamzalia Yakobo hao; nafsi zote zilikuwa 7.

26 Nafsi zote zilizomjia Yakobo na kuingia Misri zilikuwa zile zilizotoka kiunoni mwake,[s] mbali na wake za wana wa Yakobo. Nafsi zote zilikuwa 66. **27** Na wana wa Yosefu aliowazaa akiwa Misri walikuwa nafsi 2. Nafsi zote za nyumba ya Yakobo zilizokuja Misri zilikuwa 70.[t]

28 Naye akamtuma Yuda[u] mbele yake kwa Yosefu ili atoe habari kabla yake Gosheni. Kisha wakaingia nchi ya Gosheni.[v] **29** Ndipo Yosefu akatayarisha gari lake, akaenda kumpokea baba yake Israeli huko Gosheni.[w] Alipomtokea, akamwangukia shingoni mara moja, akalia shingoni

t Kut 1:5; Kum 10:22; Mdo 7:14; u Mwa 43:8; Mwa 44:18; v Mwa 45:10; Mwa 47:1; w Mwa 41:43.

pake tena na tena.[a] **30** Mwishowe Israeli akamwambia Yosefu: "Sasa niko tayari kufa,[b] kwa kuwa nimeuona uso wako, kwa maana ungali hai."

31 Kisha Yosefu akawaambia ndugu zake na watu wa nyumba ya baba yake: "Acheni niende nikamwarifu Farao, nimwambie,[c] 'Ndugu zangu na watu wa nyumba ya baba yangu waliokuwa katika nchi ya Kanaani wamekuja hapa kwangu.[d] **32** Na hao watu ni wachungaji,[e] kwa sababu walikuwa wafugaji;[f] nayo makundi yao na mifugo yao yote waliyo nayo wameleta huku.'[g] **33** Na itatukia kwamba Farao anapowaita na kuwauliza, 'Mnafanya kazi gani?' **34** Mtasema, 'Watumishi wako wamekuwa wafugaji sikuzote tangu ujana wetu mpaka sasa, sisi na pia mababu zetu,'[h] ili mpate kuishi katika nchi ya Gosheni,[i] kwa sababu kila mchungaji wa kondoo ni chukizo katika nchi ya Misri."[j]

47 Basi Yosefu akaenda, akampa Farao habari, na kusema:[k] "Baba yangu na ndugu zangu na makundi yao na mifugo yao na vyote walivyo navyo, wamekuja kutoka nchi ya Kanaani, na tazama, wako katika nchi ya Gosheni."[l] **2** Naye akatwaa watu watano kutoka kati ya ndugu zake wote apate kuwapeleka mbele ya Farao.[m]

3 Kisha Farao akawauliza ndugu zake: "Mnafanya kazi gani?"[n] Basi wakamwambia Farao: "Watumishi wako ni wachungaji wa kondoo,[o] sisi na mababu zetu pia."[p] **4** Kisha wakamwambia Farao: "Tumekuja kukaa tukiwa wageni nchini,[a] kwa sababu hakuna malisho kwa ajili ya makundi waliyo nayo watumishi wako,[b] kwa maana njaa ni kali katika nchi ya Kanaani.[c] Na sasa, tafadhali, waruhusu watumishi wako wakae katika nchi ya Gosheni."[d] **5** Ndipo Farao akamwambia Yosefu: "Baba yako na ndugu zako wamekujia hapa. **6** Nchi ya Misri iko chini ya mamlaka yako.[e] Wape makao baba yako na ndugu zako katika sehemu bora kabisa ya nchi.[f] Wape makao katika nchi ya Gosheni,[g] na ikiwa unajua kwamba kati yao mna watu walio hodari,[h] uwaweke kuwa wakuu wa mifugo yangu."[i]

7 Kisha Yosefu akamwingiza Yakobo baba yake, akamjulisha kwa Farao, naye Yakobo akambariki Farao.[j] **8** Sasa Farao akamuuliza Yakobo: "Siku za miaka ya maisha yako ni ngapi?" **9** Basi Yakobo akamwambia Farao: "Siku za miaka ya makao yangu katika nchi ya kigeni ni miaka 130.[k] Zimekuwa chache na zenye kutaabisha,[l] nazo hazijafikia siku za miaka ya maisha ya baba zangu, siku za makao yao katika nchi ya kigeni."[m] **10** Halafu Yakobo akambariki Farao na kuondoka mbele ya Farao.[n]

11 Kwa hiyo Yosefu akampa baba yake na ndugu zake makao, naye akawapa mali katika nchi ya Misri, katika sehemu bora kabisa ya nchi hiyo, katika nchi ya Ramesesi,[o] kama vile tu Farao alivyokuwa ameamuru. **12** Na Yosefu akaendelea kumpa mkate baba yake na ndugu zake na watu wote wa nyumba ya baba yake,[p] kwa kadiri ya idadi ya watoto.[q]

SURA 46
a Mwa 33:4
Mwa 45:14
b Mwa 45:28
Lu 2:29
c Mwa 41:40
d Mwa 45:19
Mwa 47:1
Mdo 7:13
e Mwa 31:18
Mwa 47:3
f Mwa 31:38
g Mwa 46:6
h Mwa 30:35
Mwa 34:5
i Mwa 45:18
Mwa 47:27
j Mwa 43:32

SURA 47
k Mwa 46:31
l Mwa 45:10
Kut 8:22
m Mdo 7:13
n Mwa 46:33
o Mwa 31:18
p Mwa 12:16
Mwa 26:14
Mwa 46:34

Safu ya 2
a Mwa 15:13
Kum 26:5
Zb 105:23
Isa 52:4
Mdo 7:6
b Yoe 1:18
c Mdo 7:11
d Mwa 45:10
e Mwa 42:34
f Mwa 13:10
Mwa 45:18
g Mwa 46:34
h Met 22:29
i 1Nya 27:31
j Kut 12:32
1Sa 13:10
2Fa 10:15
k 1Nya 29:15
Zb 39:12
Ebr 11:9
l Ayu 14:1
Yak 4:14
m Mwa 25:7
Mwa 35:28
Kut 6:4
n 2Sa 19:39
1Fa 8:66
o Mwa 45:10
Kut 1:11
Kut 12:37
Hes 33:3
p Met 11:25
1Ti 5:8
q Mwa 50:8

13 Sasa hapakuwa na mkate katika nchi yote, kwa sababu njaa ilikuwa kali sana;[a] nayo nchi ya Misri na nchi ya Kanaani zikaishiwa kabisa kwa sababu ya hiyo njaa.[b] **14** Yosefu akakusanya pesa zote zilizopatikana katika nchi ya Misri na katika nchi ya Kanaani za nafaka ambayo watu walikuwa wakinunua;[c] naye akawa akizileta pesa hizo nyumbani kwa Farao. **15** Mwishowe pesa za nchi ya Misri na za nchi ya Kanaani zikaisha, na Wamisri wote wakaanza kumjia Yosefu, wakisema: "Tupe mkate![d] Na kwa nini tufe mbele yako kwa kuwa pesa zimekwisha?"[e] **16** Kisha Yosefu akasema: "Leteni mifugo yenu nami nitawapa mkate kwa kubadilishana na mifugo yenu, ikiwa pesa zimekwisha." **17** Nao wakaanza kumletea Yosefu mifugo yao; naye Yosefu akawapa mkate kwa kubadilishana na farasi zao na makundi na mifugo na punda,[f] naye akawapa mkate kwa kubadilishana na mifugo yao yote mwaka huo.

18 Mwishowe mwaka huo ukamalizika, nao wakaanza kumjia mwaka uliofuata na kumwambia: "Hatutamficha bwana wangu lakini pesa na makundi ya wanyama wa kufugwa wameishia kwa bwana wangu.[g] Hakuna kinachosalia mbele ya bwana wangu ila miili yetu na mashamba yetu.[h] **19** Kwa nini tufe machoni pako,[i] sisi na mashamba yetu pia? Utununue sisi na mashamba yetu kwa mkate,[j] nasi pamoja na mashamba yetu tutakuwa watumwa wa Farao; na utupe mbegu ili tupate kuishi na ili tusife na mashamba yetu yasikae ukiwa."[a] **20** Basi Yosefu akamnunulia Farao mashamba yote ya Wamisri,[b] kwa sababu Wamisri waliuza kila mtu shamba lake, kwa maana ile njaa ilikuwa imewalemea sana; na hayo mashamba yakawa ya Farao.

21 Naye akawaondoa watu na kuwapeleka majijini toka mwisho mmoja wa eneo la Misri mpaka mwisho ule mwingine.[c] **22** Ni mashamba ya makuhani tu ndiyo hakuyanunua,[d] kwa sababu posho ya makuhani ilitoka kwa Farao, nao walikula posho yao waliyopewa na Farao.[e] Ndiyo sababu hawakuyauza mashamba yao.[f] **23** Kisha Yosefu akawaambia watu: "Tazameni, leo nimewanunua ninyi na mashamba yenu kwa ajili ya Farao. Mbegu zenu hizi, zipandeni katika mashamba.[g] **24** Wakati ambapo zitazaa,[h] ndipo mtampa Farao sehemu ya tano,[i] lakini sehemu nne zitakuwa zenu, ziwe mbegu za shamba na chakula chenu na cha wale walio katika nyumba zenu na cha watoto wenu."[j] **25** Basi wakasema: "Umehifadhi uhai wetu.[k] Na tupate kibali machoni pako bwana wangu, nasi tutakuwa watumwa wa Farao."[l] **26** Na Yosefu akaifanya iwe amri mpaka leo hii kuhusu mashamba yaliyo mali ya Misri ya kwamba Farao apewe mpaka sehemu ya tano. Ni mashamba ya makuhani tu wakiwa kikundi tofauti ndiyo hayakuwa ya Farao.[m]

27 Na Israeli akaendelea kukaa katika nchi ya Misri, katika nchi ya Gosheni;[n] nao wakafanya makao humo, wakaongezeka, wakawa wengi sana.[o]

SURA 47

a Mwa 41:31
b Mwa 41:30
c Mwa 41:56
Mwa 44:25
d Kut 16:3
e Mhu 7:12
Omb 1:11
f 1Fa 10:28
g Ne 5:3
h Ne 5:2
Mk 8:37
i Ayu 2:4
j Omb 4:9

Safu ya 2

a Ebr 2:15
b Met 11:26
c Mwa 41:48
Zb 33:19
Zb 107:36
d Mwa 41:45
e Ne 13:13
Mt 10:10
1Ko 9:13
f Ezr 7:24
g Mwa 45:6
Zb 41:1
2Ko 9:10
h Zb 85:12
Zb 107:37
i Mwa 41:34
1Sa 8:15
Ro 13:7
j Met 12:11
1Ti 5:18
k Mwa 45:5
Met 11:26
Mdo 7:11
l Mwa 47:19
Met 14:21
m Mwa 47:22
n Mwa 47:4
o Kut 1:7
Kum 10:22
Zb 105:24
Mdo 7:17

28 Na Yakobo akaendelea kuishi katika nchi ya Misri kwa miaka 17, hivi kwamba siku za miaka ya maisha ya Yakobo zikawa miaka 147.[a]

29 Mwishowe siku za Israeli kufa zikakaribia.[b] Basi akamwita mwana wake Yosefu, akamwambia: "Ikiwa sasa nimepata kibali machoni pako, tafadhali, weka mkono wako chini ya paja langu,[c] nawe unionyeshe fadhili zenye upendo na kweli.[d] (Tafadhali, usinizike Misri.)[e] **30** Nami nitalala pamoja na baba zangu,[f] nawe unichukue toka Misri, unizike katika kaburi lao."[g] Basi akasema: "Mimi mwenyewe nitafanya kama ulivyosema." **31** Kisha akamwambia: "Niapie." Basi akamwapia.[h] Ndipo Israeli akajilaza kifudifudi juu ya kichwa cha kitanda.[i]

48 Ikawa kwamba baada ya mambo hayo Yosefu akaambiwa: "Tazama, baba yako anadhoofika." Basi akawachukua wanawe wawili Manase na Efraimu,[j] pamoja naye. **2** Kisha Yakobo akaambiwa: "Tazama, mwana wako Yosefu amekuja kwako." Basi Israeli akajikaza akaketi kitandani mwake. **3** Naye Yakobo akamwambia Yosefu:

"Mungu Mweza-Yote alinitokea Luzi[k] katika nchi ya Kanaani apate kunibariki.[l] **4** Naye akaniambia, 'Tazama, nakufanya uzae,[m] nami nitakufanya kuwa wengi na nitakufanya uwe kutaniko la vikundi vya watu,[n] nami nitaupa uzao wako baada yako nchi hii iwe miliki mpaka wakati usio na kipimo.'[o] **5** Na sasa wana wako wawili waliozaliwa katika nchi ya Misri kabla sijaja hapa kwako Misri ni wangu.[a] Efraimu na Manase watakuwa wangu kama vile Rubeni na Simeoni.[b] **6** Lakini watoto wako utakaozaa baada ya hawa watakuwa wako. Pamoja na majina ya ndugu zao wataitwa katika urithi wao.[c] **7** Nami, nilipokuwa nikija kutoka Padani,[d] Raheli alikufa[e] kando yangu njiani katika nchi ya Kanaani wakati kulipokuwa kungali mwendo mkubwa kabla ya kufika Efrathi,[f] basi nikamzika huko kwenye njia ya kwenda Efrathi, yaani, Bethlehemu."[g]

8 Kisha Israeli akawaona wana wa Yosefu, akauliza: "Ni nani hawa?"[h] **9** Yosefu akamwambia baba yake: "Hawa ndio wanangu ambao Mungu amenipa nikiwa mahali hapa."[i] Basi akasema: "Tafadhali, walete kwangu nipate kuwabariki."[j] **10** Sasa macho ya Israeli yalikuwa yamefifia kutokana na uzee.[k] Hakuweza kuona. Basi akawaleta karibu naye, naye akawabusu na kuwakumbatia.[l] **11** Na Israeli akamwambia Yosefu: "Sikuwaza ningeuona uso wako,[m] lakini tazama, Mungu ameniruhusu nione uzao wako pia." **12** Kisha Yosefu akawatoa katika magoti yake, naye akainama kifudifudi.[n]

13 Yosefu akawachukua sasa wote wawili, Efraimu kwa mkono wake wa kuume ukiwa upande wa mkono wa kushoto wa Israeli,[o] na Manase kwa mkono wake wa kushoto ukiwa upande wa mkono wa kuume wa Israeli,[p] akawaleta karibu naye. **14** Lakini, Israeli akaunyoosha mkono wake wa kuume na kuuweka juu ya kichwa

SURA 47

a Mwa 47:9
b Mwa 49:33
Ebr 11:21
c Mwa 24:9
d Mwa 24:49
e Mwa 46:4
Mwa 50:13
Mdo 7:16
f Mwa 49:33
g Mwa 25:9
Mwa 49:29
h Mwa 50:5
i 1Fa 1:47
Ebr 11:21

SURA 48

j Mwa 41:50
Yos 14:4
k Mwa 28:19
l Mwa 28:13
Ho 12:4
m Mwa 28:14
Mwa 32:12
n Mwa 28:3
Mwa 35:11
Mdo 7:17
o Mwa 28:13
Kum 32:8
Amo 9:15
Mdo 7:5

Safu ya 2

a Yos 14:4
1Nya 5:1
b Mwa 35:23
c Yos 13:29
Yos 16:5
Zb 77:15
d Mwa 33:18
Ho 12:12
e Mwa 35:19
f Ru 4:11
Mik 5:2
g 1Sa 17:12
Mt 2:6
h Mwa 27:18
i Mwa 41:50
j Mwa 27:4
Mwa 28:1
Kum 33:1
Ebr 11:21
k Mwa 27:1
Mhu 12:3
l Mwa 27:26
m Mwa 37:35
Mwa 42:36
Mwa 46:30
n Mwa 18:2
Mwa 33:3
o Mwa 41:52
p Mwa 41:51
Zb 89:13
Mdo 2:34
Efe 1:20

cha Efraimu,[a] ingawa ndiye
aliyekuwa mdogo,[b] nao mko-
no wake wa kushoto juu ya
kichwa cha Manase.[c] Aliiwe-
ka mikono yake hivyo kwa
makusudi, kwa kuwa Manase
ndiye aliyekuwa mzaliwa wa
kwanza.[d] **15** Naye akambari-
ki Yosefu na kusema:[e]

"Mungu wa kweli ambaye
mbele zake baba zangu
Abrahamu na Isaka
walitembea,[f]
Mungu wa kweli ambaye
amekuwa akinichunga
maisha yangu yote
mpaka leo hii,[g]
16 Malaika ambaye amekuwa
akiniponya katika misiba
yote,[h] awabariki
wavulana hawa.[i]
Na jina langu liitwe juu yao
na pia jina la baba zangu,
Abrahamu na Isaka,[j]
Na waongezeke wawe
wengi katikati ya
dunia."[k]

17 Yosefu alipoona kwamba
baba yake aliuweka mkono
wake wa kuume juu ya kichwa
cha Efraimu, hakupendezwa,[l]
naye akajaribu kuushika mko-
no wa baba yake auondoe juu
ya kichwa cha Efraimu na kuu-
weka juu ya kichwa cha Mana-
se.[m] **18** Kwa hiyo Yosefu aka-
mwambia baba yake: "Sivyo,
baba yangu, kwa sababu huyu
ndiye mzaliwa wa kwanza.[n]
Uweke mkono wako wa kuume
juu ya kichwa chake." **19** La-
kini baba yake akaendelea ku-
kataa, akisema: "Najua, mwa-
nangu, najua. Yeye pia ataku-
wa kikundi cha watu naye pia
atakuwa mkuu.[o] Lakini, ndugu
yake mdogo atakuwa mkuu ku-
liko yeye,[p] nao uzao wake uta-
kuwa hesabu kamili ya matai-
fa."[a] **20** Naye akaendelea ku-
wabariki siku hiyo,[b] akisema:

"Kupitia kwako Israeli na
atangaze baraka tena na
tena, akisema,
'Mungu na akufanye wewe
uwe kama Efraimu na
kama Manase.'"[c]

Hivyo akaendelea kumweka
Efraimu mbele ya Manase.[d]
21 Kisha Israeli akamwa-
mbia Yosefu: "Tazama, ninaku-
fa,[e] lakini Mungu pasipo shaka
ataendelea kuwa nanyi na ku-
warudisha ninyi katika nchi ya
mababu zenu.[f] **22** Nami, ni-
nakupa sehemu moja ya
nchi zaidi kuliko ndugu zako,[g]
ambayo niliichukua kutoka ka-
tika mkono wa Waamori, kwa
upanga wangu na kwa upinde
wangu."

49 Baadaye Yakobo akawa-
ita pamoja wanawe, aka-
sema: "Jikusanyeni pamoja ni-
waambie yatakayowapata siku
za mwisho. **2** Jikusanyeni
msikilize, ninyi wana wa Ya-
kobo, ndiyo, msikilizeni Israeli
baba yenu.[h]
3 "Rubeni, wewe ndiwe mza-
liwa wangu wa kwanza,[i] ngu-
vu zangu na mwanzo wa ngu-
vu zangu za uzazi,[j] ubora wa
heshima na ubora wa nguvu.
4 Umeruka mpaka kama maji,
basi usiwe na ukuu,[k] kwa sa-
babu umekipanda kitanda cha
baba yako.[l] Wakati huo ulikina-
jisi kitanda changu.[m] Aliki-
panda!
5 "Simeoni na Lawi ni ndu-
gu.[n] Silaha zao za kuchinjia ni
vyombo vya jeuri.[o] **6** Ee nafsi
yangu, usiingie katika kikundi
chao cha rafiki.[p] Ee mwelekezo
wangu, usiungane na kutaniko
lao,[q] kwa sababu katika hasira

SURA 48
a Kut 15:6
Zb 110:1
1Pe 3:22
Ufu 1:17
b Mwa 25:23
c Mk 10:16
d Mwa 41:51
Mwa 46:20
e 1Nya 5:2
f Mwa 17:1
Mwa 24:40
g Mwa 28:13
Zb 23:1
1Pe 2:25
h Mwa 28:15
Mwa 31:11
Kut 15:13
Ayu 19:25
Zb 34:7
i Mwa 32:26
j Mwa 32:28
Isa 44:5
k Kut 1:7
Hes 26:34
Hes 26:37
l Ro 9:16
m 1Sa 16:7
n Mwa 41:51
Kum 21:17
o Mwa 17:20
p Hes 2:19
Hes 2:21

Safu ya 2
a Mwa 25:23
Hes 1:33
Hes 1:35
Kum 33:17
Yer 31:9
b Ebr 11:21
c Kum 10:22
d Kum 33:17
Kum 34:2
Yos 17:17
e Mwa 50:24
f Mwa 15:14
Mwa 26:3
Kum 31:8
g Kum 21:17
Yos 17:14
Eze 47:13

SURA 49
h Mwa 49:28
i Mwa 29:32
Kut 6:14
1Nya 5:1
j Kum 21:17
Zb 78:51
k Kum 33:6
l Mwa 35:22
m Law 18:8
Kum 27:20
1Ko 5:1
n Mwa 29:33
Mwa 29:34
Mwa 35:23
o Mwa 34:25
p Zb 64:2
q Zb 26:5

yao waliwaua watu,[a] na katika
udhalimu wao walikata mishi-
pa ya ng'ombe-dume. **7** Na
ilaaniwe hasira yao,[b] kwa saba-
bu ni katili,[c] na ghadhabu yao,
kwa sababu hutenda kwa uka-
li.[d] Acheni niwagawanye katika
Yakobo na kuwatawanya kati-
ka Israeli.[e]

8 "Yuda,[f] nawe, ndugu zako
watakusifu.[g] Mkono wako uta-
kuwa katika kikosi cha adui
zako.[h] Wana wa baba yako wa-
tajilaza kifudifudi mbele yako.[i]
9 Yuda ni mwana-simba.[j] Mwa-
nangu, utapanda kutoka ma-
windoni. Aliinama, alijinyoosha
kama simba, na kama simba,
ni nani anayethubutu ku-
mwamsha?[k] **10** Fimbo ya enzi
haitageuka kando kutoka
kwa Yuda,[l] wala fimbo ya kio-
ngozi kutoka katikati ya mi-
guu yake, mpaka Shilo aje;[m]
na vikundi vya watu vitamtii
yeye.[n] **11** Kwa kumfunga pu-
nda wake mkomavu kwenye
mzabibu na mwana-punda wake
mwenyewe kwenye mzabibu
mzuri, yeye kwa hakika ata-
fua mavazi yake katika divai na
vazi lake katika damu ya zabi-
bu.[o] **12** Macho yake ni meku-
ndu kwa divai, na weupe wa
meno yake unatokana na ma-
ziwa.

13 "Zabuloni atakaa kando
ya bahari,[p] naye atakuwa ka-
ndo ya bahari ambapo meli hu-
kaa zikiwa zimetia nanga;[q] na
sehemu yake ya mbali itakuwa
kuelekea Sidoni.[r]

14 "Isakari[s] ni punda mwe-
nye mifupa migumu, aliyela-
la katikati ya matandiko ye-
nye mifuko miwili. **15** Naye
ataona kwamba mahali pa ku-
pumzika ni pazuri na kwamba
nchi ni yenye kupendeza; naye
atainamisha bega lake abebe
mizigo naye atalazimishwa ku-
fanya kazi ya kitumwa.

16 "Dani atawahukumu watu
wake akiwa mmoja wa maka-
bila ya Israeli.[a] **17** Dani na
awe nyoka kando ya bara-
bara, nyoka-bafe kando ya njia,
anayeuma visigino vya fara-
si hivi kwamba mpandaji wake
anaanguka nyuma.[b] **18** Kwa
kweli nitaungoja wokovu kuto-
ka kwako, Ee Yehova.[c]

19 "Naye Gadi, atavamiwa
na kikundi cha waporaji, lakini
yeye atavamia upande wa nyu-
ma kabisa.[d]

20 "Kutoka Asheri mkate
wake utakuwa mnono,[e] naye
atatoa vitu bora vya mfalme.[f]

21 "Naftali[g] ni paa mwemba-
mba. Anatoa maneno ya kupe-
ndeza.[h]

22 "Yosefu ni chipukizi la
mti unaozaa matunda,[i] chipuki-
zi la mti unaozaa matunda ka-
ndo ya chemchemi,[j] ambao hu-
sukuma mbele matawi yake juu
ya ukuta.[k] **23** Lakini wapi-
ga-mishale waliendelea kumsu-
mbua na kumfyatulia mishale
na kuendelea kudumisha uadui
kumwelekea.[l] **24** Na hata hi-
vyo upinde wake ulikuwa kati-
ka mahali pa kudumu,[m] na ngu-
vu za mikono yake zilikuwa
zenye kunepa.[n] Kwa mikono
ya Mwenye Nguvu wa Yako-
bo,[o] hapo ndipo alipo Mchunga-
ji, Jiwe la Israeli.[p] **25** Yeye
ametoka kwa Mungu wa baba
yako,[q] naye atakusaidia;[r] naye
yuko pamoja na Mweza-Yote,[s]
naye atakubariki kwa baraka
za mbingu zilizo juu,[t] kwa ba-
raka za kilindi cha maji kilicho

SURA 49

a Mwa 34:7
Ro 12:19
b Met 22:24
Efe 4:31
c Met 11:17
d Mwa 34:25
e Yos 19:1
Yos 21:41
f Mwa 29:35
g Mwa 43:9
Mwa 46:28
1Nya 5:2
h Yos 10:24
Amu 1:2
2Sa 22:41
i Hes 10:14
Kum 33:7
2Sa 5:3
j Ho 5:14
Ufu 5:5
k Hes 24:9
l Hes 24:17
2Sa 2:4
2Sa 7:16
m Isa 9:6
Eze 21:27
Lu 1:32
Ebr 7:14
n Kum 18:18
Zb 2:8
Isa 11:10
Mt 2:6
Yoh 10:16
Ufu 7:9
o Isa 63:2
p Kum 33:19
Isa 9:1
q Mt 4:13
r Yos 19:10
s Kum 33:18
Yos 19:17
1Nya 7:5

Safu ya 2

a Amu 13:2
Amu 13:24
Amu 15:20
b Kum 33:22
Amu 14:19
Amu 15:15
c Zb 14:7
d Kum 33:20
Yos 13:8
e Kum 32:14
Zb 81:16
f Kum 33:24
Yos 19:24
1Fa 4:7
1Fa 4:16
g Kum 33:23
Yos 19:32
Mt 4:15
h Mt 4:13
Yoh 7:46
i Kut 1:5
j Kum 33:13
Yos 16:1
k Kum 33:17
l Mwa 37:8
Mwa 40:15
m Mwa 50:20
n Hes 13:8
Yos 1:6
Yos 8:18
Amu 6:14
Amu 11:32
o Zb 80:1
p Mwa 45:7
Mwa 50:20
Isa 28:16
Mt 21:42
1Pe 2:4
q Yoh 17:3
r Flp 4:19
s Ebr 10:12
t Mal 3:10

chini,[a] kwa baraka za maziwa
na tumbo la uzazi.[b] **26** Baraka
za baba yako kwa kweli zitaku-
wa kuu kuliko baraka za milima
ya milele,[c] kuliko pambo la vili-
ma vinavyodumu mpaka waka-
ti usio na kipimo.[d] Zitaendelea
kuwa juu ya kichwa cha Yosefu,
ndiyo, juu ya utosi wa kichwa
cha yule aliyetengwa na ndugu
zake.[e]

27 "Benyamini ataendelea
kurarua kama mbwa-mwitu.[f]
Asubuhi atakula mnyama ali-
yekamatwa na jioni atagawa-
nya nyara."[g]

28 Yote hayo ndiyo makabi-
la kumi na mawili ya Israeli,
na hayo ndiyo maneno amba-
yo baba yao aliwaambia alipo-
kuwa akiwabariki. Alimbariki
kila mmoja kupatana na bara-
ka yake.[h]

29 Kisha akawaamuru na
kuwaambia: "Mimi ninakusa-
nywa kwa watu wangu.[i] Nizi-
keni pamoja na baba zangu ka-
tika pango lililo katika sha-
mba la Efroni Mhiti,[j] **30** kati-
ka pango lililo katika shamba
la Makpela mbele ya Mamre
katika nchi ya Kanaani, sha-
mba ambalo Abrahamu alinu-
nua kutoka kwa Efroni Mhi-
ti awe na mahali pa kuzikia.[k]
31 Huko walimzika Abrahamu
na Sara mke wake.[l] Huko wa-
limzika Isaka na Rebeka mke
wake,[m] na huko nilimzika Lea.
32 Shamba lililonunuliwa na
pango lililo ndani yake lilitoka
kwa wana wa Hethi."[n]

33 Basi Yakobo akamaliza
kuwapa wanawe amri. Kisha
akaiweka miguu yake pamoja
juu ya kitanda, akakata pumzi,
akakusanywa kwa watu wake.[o]

SURA 49
a Kum 33:13
Isa 11:9
b Isa 59:21
c Yos 17:14
d Isa 54:10
e Kum 33:16
Mdo 7:9
f Kum 33:12
Amu 20:16
1Sa 9:16
g Est 2:5
Est 8:7
h Ebr 11:21
i Mwa 35:29
Mwa 49:33
j Mwa 23:17
k Mwa 23:20
l Mwa 23:19
Mwa 25:10
m Mwa 35:29
n Mwa 23:18
o Mwa 25:8
Zb 116:15
Mt 22:32
Mdo 7:15

Safu ya 2

SURA 50
a Mwa 46:4
b Mhu 7:2
Yoh 11:35
Mdo 8:2
c Mwa 50:26
d Hes 20:29
e Mwa 18:3
f Mwa 47:31
Mt 5:33
Ebr 6:16
g Mwa 48:21
1Ko 15:22
h Mwa 23:17
Mwa 49:30
i Mwa 46:4
Mwa 47:29
Yoh 19:38
j Mwa 47:31
k Zb 105:22
Mdo 4:8
l Mwa 32:5
Mwa 46:27
m Mwa 41:43
Mwa 46:29
Mdo 8:28

50 Ndipo Yosefu akauangu-
kia uso wa baba yake,[a]
akamlilia na kumbusu.[b] **2** Ki-
sha Yosefu akawaamuru watu-
mishi wake, matabibu, wampa-
ke baba yake dawa ya kumfa-
nya asioze.[c] Basi wakampaka
Israeli dawa ya kumfanya asio-
ze, **3** nao wakatumia siku 40
kamili kwa ajili yake, kwa ma-
ana hiyo ndiyo hesabu ya siku
ambazo kwa desturi wao hutu-
mia kupaka dawa ya kumfanya
mtu asioze, nao Wamisri waka-
endelea kumlilia siku 70.[d]

4 Mwishowe siku za kumli-
lia zikapita, na Yosefu akawa-
ambia watu wa nyumba ya Fa-
rao, akisema: "Ikiwa, sasa, ni-
mepata kibali machoni penu,[e]
tafadhali, nendeni mkaseme
masikioni mwa Farao, na ku-
mwambia, **5** 'Baba yangu ali-
niapisha,[f] akisema: "Tazama!
Ninakufa.[g] Katika kaburi
ambalo nimechimba mwenyewe
katika nchi ya Kanaani[h] ndipo
utakaponizika."[i] Na sasa, tafa-
dhali, niruhusu niende huko, ni-
kamzike baba yangu, kisha nita-
rudi.'" **6** Basi Farao akasema:
"Nenda ukamzike baba yako
kama alivyokuapisha."[j]

7 Kwa hiyo Yosefu akaenda
kumzika baba yake, na watu-
mishi wote wa Farao, wanau-
me wazee[k] wa nyumba yake na
wanaume wote wazee wa nchi
ya Misri, wakapanda kwenda
pamoja naye, **8** na watu wote
wa nyumba ya Yosefu na ndu-
gu zake na nyumba ya baba
yake.[l] Waliacha tu katika nchi
ya Gosheni watoto wao wado-
go na makundi yao na mifugo
yao. **9** Pia magari[m] na wapa-
nda-farasi walienda pamoja
naye, nayo kambi ikawa na ida-

di kubwa sana. **10** Kisha wa-
kafika kwenye uwanja wa ku-
puria[a] wa Atadi, ulio katika
eneo la Yordani,[b] na huko wa-
kaomboleza maombolezo ma-
kuu sana na kulia sana, naye
akafanya desturi za kuombole-
za kwa ajili ya baba yake kwa
siku saba.[c] **11** Nao wakaaji
wa nchi hiyo, Wakanaani, wa-
kaona desturi za kuomboleza
katika uwanja wa kupuria wa
Atadi, nao wakasema: "Haya ni
maombolezo makuu ya Wami-
sri!" Ndiyo sababu mahali hapo
paliitwa Abel-misraimu, palipo
katika eneo la Yordani.[d]

12 Nao wanawe wakamfa-
nyia kama vile tu alivyokuwa
amewaamuru.[e] **13** Kwa hiyo
wanawe wakampeleka mpa-
ka nchi ya Kanaani na ku-
mzika katika pango la shamba
la Makpela, shamba ambalo
Abrahamu alikuwa amenunua
kutoka kwa Efroni Mhiti mbe-
le ya Mamre[f] ili awe na maha-
li pa kuzikia. **14** Baada ya ku-
mzika baba yake, Yosefu aka-
rudi Misri, yeye na ndugu zake
na wale wote waliokwenda pa-
moja naye kumzika baba yake.

15 Ndugu za Yosefu walipo-
ona kwamba baba yao ameku-
fa, wakaanza kusema: "Hue-
nda ikawa Yosefu anatuwe-
kea uadui[g] naye hakika ata-
tulipiza kwa sababu ya uovu
wote ambao tumemtendea."[h]
16 Basi wakamjulisha Yose-
fu amri kwa maneno haya:
"Baba yako alitoa amri hii ka-
bla ya kifo chake, akisema,
17 'Mtamwambia Yosefu hivi:
"Tafadhali, nakuomba, usame-
he[i] maasi ya ndugu zako na
dhambi yao kwa kuwa wame-
kutendea uovu."'[j] Na tafadha-
li sasa, usamehe maasi ya wa-
tumishi wa Mungu wa baba
yako."[a] Naye Yosefu akalia wali-
posema naye. **18** Halafu ndu-
gu zake pia wakaja na kuangu-
ka chini mbele yake. Wakamwa-
mbia: "Tazama, sisi ni kama
watumwa kwako!"[b] **19** Ndipo
Yosefu akawaambia: "Msiogope,
kwa maana je, mimi niko ma-
hali pa Mungu?[c] **20** Kwa upa-
nde wenu, ninyi mlikuwa na
uovu akilini mwenu kuniele-
kea mimi. Mungu alikuwa na
wema akilini kwa kusudi la
kutenda kama ilivyo leo hii
ili kuhifadhi hai watu we-
ngi.[d] **21** Kwa hiyo sasa msio-
gope. Mimi nitaendelea kuwa-
pa chakula ninyi na watoto
wenu wadogo."[e] Basi akawafa-
riji na kusema nao kwa kuwa-
tuliza.

22 Na Yosefu akaendelea ku-
kaa Misri, yeye na nyumba ya
baba yake; na Yosefu akaishi mi-
aka mia moja na kumi. **23** Na
Yosefu akapata kuona wana
wa Efraimu wa kizazi cha tatu,[f]
pia wana wa Makiri,[g] mwana
wa Manase. Walizaliwa juu ya
magoti ya Yosefu.[h] **24** Mwi-
showe Yosefu akawaambia ndu-
gu zake: "Ninakufa; lakini Mu-
ngu hatakosa kuwaelekezea fi-
kira zake,[i] naye kwa hakika
atawatoa katika nchi hii na ku-
wapeleka mpaka nchi ambayo
aliwaapia Abrahamu, Isaka na
Yakobo."[j] **25** Basi Yosefu aka-
waapisha wana wa Israeli, aki-
sema: "Mungu hatakosa kuwa-
elekezea fikira zake. Kwa hiyo
mwichukue mifupa yangu ku-
toka huku."[k] **26** Kisha Yosefu
akafa akiwa na umri wa miaka
mia moja na kumi; nao waka-
mpaka dawa ya kumfanya asi-
oze,[l] naye akatiwa ndani ya sa-
nduku huko Misri.

SURA 50
a Mt 3:12
b Kum 1:1
c 1Sa 31:13
Mk 5:38
d Mwa 10:19
e Mwa 47:29
Mwa 49:29
Efe 6:1
f Mwa 23:17
Mwa 25:9
Mwa 35:27
Mwa 49:30
g Mwa 27:41
Law 19:17
Met 19:11
Met 28:1
h Mwa 37:28
Mwa 42:21
Zb 105:17
Met 24:29
Lu 17:3
Ro 12:17
1Ko 13:5
i Mt 6:12
Mt 18:35
Lu 17:3
Efe 4:32
j Mwa 37:28
1Sa 24:17
Met 28:13
Ro 13:10

Safu ya 2
a 2Ko 7:10
b Mwa 37:7
Efe 6:7
c Kum 32:35
Ro 12:19
d Mwa 37:18
Mwa 45:5
Zb 105:17
Zb 119:71
Ro 8:28
e Mwa 47:12
1Pe 3:9
f 1Nya 7:20
g Yos 17:1
1Nya 7:14
h Mwa 30:3
i Kut 4:31
j Mwa 12:7
Mwa 17:8
Mwa 26:3
Mwa 28:13
k Kut 13:19
Yos 24:32
Ebr 11:22
l Mwa 50:2

KUTOKA

1 Na haya ndiyo majina ya
wana wa Israeli walioingia
Misri pamoja na Yakobo; walio-
ingia kila mwanamume na nyu-
mba yake:[a] **2** Rubeni,[b] Simeo-
ni,[c] Lawi[d] na Yuda,[e] **3** Isaka-
ri,[f] Zabuloni[g] na Benyami-
ni,[h] **4** Dani[i] na Naftali,[j] Gadi[k]
na Asheri.[l] **5** Nafsi zote zili-
zotoka katika kiuno[m] cha Ya-
kobo zikawa nafsi 70, lakini
tayari Yosefu alikuwa Misri.[n]
6 Mwishowe Yosefu akafa,[o] na
pia ndugu zake wote na kiza-
zi hicho chote. **7** Na wana wa
Israeli wakazaa na kuanza ku-
jaa; nao wakazidi kuongeze-
ka na kuwa wenye nguvu zai-
di kwa kiwango kisicho cha ka-
waida, hivi kwamba wakaijaza
nchi.[p]

8 Baada ya muda mfalme
mpya ambaye hakumjua Yo-
sefu akainuka juu ya Misri.[q]
9 Naye akawaambia watu wake:
"Tazama! Watu wa wana wa Isra-
eli ni wengi zaidi na wenye ngu-
vu kuliko sisi.[r] **10** Haya! Na
tuwatendee kwa werevu,[s] wasi-
je wakaongezeka, na iwe kwa-
mba, vita vikizuka juu yetu,
basi hakika wao watajiunga na
wale wanaotuchukia na kupiga-
na nasi na kutoka katika nchi
hii."

11 Basi wakaweka juu yao
wakuu wa kazi ya kulazimi-
shwa kusudi wawakandamize
katika kazi yao ya kubeba mi-
zigo;[t] nao wakajenga majiji ili
yawe maghala kwa ajili ya Fa-
rao, yaani, Pithomu na Raam-
sesi.[u] **12** Lakini kadiri wali-
vyowakandamiza, ndivyo wali-
vyozidi kuongezeka na ndivyo
walivyozidi kuenea kotekote,

SURA 1

a Mwa 46:8
b Kut 6:14
c Kut 6:15
d Kut 2:1
Kut 6:16
e 1Nya 2:3
Ebr 7:14
f Mwa 46:13
g Mwa 46:14
h Mwa 46:21
i Mwa 46:23
j 1Nya 7:13
k Mwa 46:16
l 1Nya 7:30
m Mwa 46:26
n Kum 10:22
Mdo 7:14
o Mwa 50:26
p Mwa 46:3
Kum 26:5
Mdo 7:17
q Mdo 7:18
r Hes 22:3
Zb 105:24
s Zb 105:25
Met 21:30
Mdo 7:19
1Ko 3:19
t Mwa 15:13
Kut 3:7
Hes 20:15
Kum 26:6
Mdo 7:34
u Mwa 47:11

Safu ya 2

a Zb 105:24
Zb 105:38
b Kut 2:23
Met 14:31
Mdo 7:6
c Nah 3:14
d Kut 5:7
Zb 81:6
e Kut 20:2
Law 25:43
Law 26:13
Met 29:2
Isa 14:6
f Mwa 35:17
Mwa 38:28
Eze 16:4
g Ne 5:15
Met 8:13
h Da 3:16
Da 6:13
Mt 10:28
Mdo 5:29
i Mwa 9:6
j Mhu 8:4
k Zb 41:2
Met 11:18
Met 19:17
Mhu 8:12
Isa 3:10
Lu 1:50
Ebr 6:10

hivi kwamba wakahofu na ku-
chukizwa kwa sababu ya wana
wa Israeli.[a] **13** Kwa hiyo Wa-
misri wakawatumikisha wana
wa Israeli chini ya uonevu.[b]
14 Nao wakazidi kuyafanya
maisha yao yawe machungu
kwa utumwa mgumu wa kute-
ngeneza saruji ya udongo[c] na
matofali na kwa kila namna ya
utumwa shambani,[d] ndiyo, kila
namna ya utumwa wao ambao
kwa huo waliwatumia wakiwa
watumwa chini ya uonevu.[e]

15 Baadaye mfalme wa Mi-
sri akawaambia wazalishaji[f]
Waebrania, ambao jina la mmo-
ja wao lilikuwa Shifra na jina
la yule mwingine lilikuwa Pua,
16 ndiyo, hata akawaambia:
"Mnapowasaidia wanawake Wa-
ebrania kuzaa nanyi mpate ku-
waona kwenye kiti cha kuzalia,
ikiwa ni mtoto wa kiume, mu-
ueni; lakini ikiwa ni binti, basi
na aishi." **17** Hata hivyo, wa-
zalishaji hao walimwogopa Mu-
ngu wa kweli,[g] nao hawakufa-
nya kama vile mfalme wa Mi-
sri alivyokuwa amewaambia,[h]
bali walikuwa wakiwahifadhi
hai watoto wa kiume.[i] **18** Baa-
da ya muda mfalme wa Misri
akawaita wazalishaji hao na ku-
waambia: "Kwa nini mmefanya
jambo hili, ya kwamba mliwa-
hifadhi hai watoto wa kiume?"[j]
19 Nao wazalishaji wakamwa-
mbia Farao: "Kwa sababu wana-
wake Waebrania si kama wana-
wake Wamisri. Kwa sababu wao
ni wenye nguvu, wao huwa taya-
ri wamezaa kabla mzalishaji ha-
jaingia kwao."

20 Kwa hiyo Mungu akawa-
tendea vema wazalishaji hao;[k]

na watu wakazidi kuongezeka
na kuwa wengi zaidi na kuwa
wenye nguvu sana. **21** Na ika-
wa kwamba kwa sababu wazali-
shaji walikuwa wamemwogopa
Mungu wa kweli, baadaye aka-
wapa familia.[a] **22** Mwishowe
Farao akawaamuru watu wake
wote, na kusema: "Kila mwana
anayezaliwa mtamtupa kwe-
nye mto Nile, lakini kila binti
mtamhifadhi hai."[b]

2 Wakati huohuo, mwanamu-
me fulani wa nyumba ya
Lawi alimchukua binti mmoja
wa Lawi.[c] **2** Naye mwanamke
huyo akapata mimba, akazaa
mwana. Alipoona jinsi alivyo-
kuwa mwenye sura ya kupe-
ndeza, akamficha[d] kwa miezi
mitatu.[e] **3** Alipokuwa hawezi
tena kuendelea kumficha,[f] aka-
mchukulia safina ya mafunjo,
akaipaka lami na bereu,[g] aka-
mweka mtoto huyo ndani yake
na kuiweka katikati ya matete[h]
kando ya mto Nile. **4** Na zaidi
ya hayo, dada yake akasimama
umbali fulani apate kuona kile
ambacho angetendewa.[i]

5 Baada ya muda, binti ya
Farao akaja kuoga katika Mto
Nile, nao wanawake wa kumhu-
dumia walikuwa wakitembea
kando ya Mto Nile. Naye akaio-
na ile safina katikati ya matete.
Mara moja akamtuma kijaka-
zi wake aende akailete.[j] **6** Ali-
poifungua akamwona yule mto-
to, na tazama, mvulana huyo
alikuwa akilia. Kwa hiyo aka-
mwonea huruma,[k] ingawa ali-
sema: "Huyu ni mmoja wa wa-
toto wa Waebrania." **7** Kisha
dada ya mtoto huyo akamwa-
mbia binti ya Farao: "Je, nie-
nde nikakuitie mwanamke ana-
yenyonyesha kutoka kati ya
wanawake Waebrania apate
kukunyonyeshea mtoto huyu?"
8 Basi binti ya Farao akamwa-
mbia: "Nenda!" Naye mwana-
mwali huyo akaenda mara moja
na kumwita mama ya mtoto
huyo.[a] **9** Ndipo binti ya Farao
akamwambia: "Mchukue mto-
to huyu, uninyonyeshee, nami
nitakupa malipo[b] yako." Kwa
hiyo mwanamke huyo aka-
mchukua mtoto na kumnyo-
nyesha. **10** Naye mtoto aka-
kua. Kisha akamleta kwa bi-
nti ya Farao, hivi kwamba
akawa mwana kwake;[c] naye
akamwita jina lake Musa na
kusema: "Ni kwa sababu nime-
mtoa majini."[d]

11 Sasa ikawa kwamba ka-
tika siku hizo, Musa alipozi-
di kuwa na nguvu, akatoka nje
kwenda kwa ndugu zake apa-
te kutazama mizigo waliyoku-
wa wakibeba;[e] naye akamwona
Mmisri fulani akimpiga Mwe-
brania fulani, mmoja wa ndu-
gu zake.[f] **12** Kwa hiyo aka-
tazama huku na huku akao-
na kwamba hapakuwa na mtu
yeyote karibu. Kisha akampiga
Mmisri huyo na kumuua, hala-
fu akamficha ndani ya mcha-
nga.[g]

13 Hata hivyo, akatoka siku
iliyofuata, na tazama, wana-
ume wawili Waebrania waliku-
wa wakipambana. Basi akamwa-
mbia mwenye kosa: "Kwa nini
umpige mwenzako?"[h] **14** Naye
akamwambia: "Ni nani aliyeku-
weka wewe rasmi kuwa mkuu
na mwamuzi juu yetu?[i] Je, una-
kusudia kuniua kama vile uli-
vyomuua yule Mmisri?"[j] Sasa
Musa akaogopa na kusema: "Ha-
kika jambo hilo limejulikana!"[k]

15 Baadaye Farao akasikia
juu ya jambo hilo, naye aka-
jaribu kumuua Musa;[l] lakini
Musa akakimbia[m] toka kwa

SURA 1
a Zb 107:41
Zb 127:3
b Zb 105:25
Mt 2:16
Mdo 7:19

SURA 2
c Kut 6:20
Hes 26:59
d 2Fa 11:2
e Mdo 7:20
Ebr 11:23
f Mdo 7:19
g Mwa 6:14
Mwa 14:10
h Ayu 8:11
i Kut 15:20
1Nya 6:3
Mik 6:4
j Mdo 7:21
k 1Fa 8:50
Zb 106:46
1Pe 3:8

Safu ya 2
a Kut 6:20
b 1Ti 5:18
c Ebr 11:24
d Mdo 7:21
e Kut 1:11
Kut 3:7
Mdo 7:23
f Kut 5:14
g Mdo 7:24
Ebr 11:24
h Mwa 13:8
Mdo 7:26
i Hes 16:13
Mdo 7:27
j Mdo 7:28
k Met 19:12
l Kut 4:19
m Met 22:3
Ebr 11:27

Farao apate kuishi katika nchi
ya Midiani;[a] naye akaketi kan-
do ya kisima. **16** Sasa kuha-
ni[b] wa Midiani alikuwa na bi-
nti saba, na kama kawaida wa-
kaja kuteka maji na kuijaza
mifereji ili kulinywesha ku-
ndi la baba yao.[c] **17** Na
kama kawaida wachungaji
wakaja na kuwafukuzia mba-
li. Kwa hiyo Musa akasima-
ma na kuwasaidia wanawake
hao na kulinywesha kundi lao.[d]
18 Basi walipofika nyumbani
kwa Reueli[e] baba yao, akase-
ma kwa mshangao: "Imeku-
waje mmefika nyumbani upesi
sana leo?" **19** Nao wakasema:
"Mmisri[f] fulani alitukomboa
kutoka katika mkono wa wa-
chungaji na, zaidi ya hayo, kwa
kweli alitutekea maji ili kuli-
nywesha kundi." **20** Kisha
akawaambia binti zake: "Laki-
ni yeye yuko wapi? Kwa nini
mmemwacha nyuma mwana-
mume huyo? Mwiteni, apate
kula mkate."[g] **21** Baada ya
hayo Musa akakubali kukaa
na mtu huyo, naye aka-
mpa Musa Sipora[h] binti yake.
22 Baadaye Sipora akazaa
mwana, naye Musa akamwita
jina lake Gershomu,[i] kwa saba-
bu, alisema: "Nimekuwa mkaaji
mgeni katika nchi ya kigeni."[j]

23 Na ikawa kwamba waka-
ti wa siku hizo nyingi, mwisho-
we mfalme wa Misri akafa,[k] la-
kini wana wa Israeli wakaende-
lea kuugua kwa sababu ya utu-
mwa na kulia kwa kulalamika,[l]
nacho kilio chao cha kuomba
msaada kikaendelea kupaa juu
kwa Mungu wa kweli kwa saba-
bu ya utumwa huo.[m] **24** Mwi-
showe Mungu akasikia[n] kuugua[o]
kwao naye Mungu akali-
kumbuka agano lake pamoja
na Abrahamu, Isaka na Yako-
bo.[a] **25** Basi Mungu akawatazama wana wa Israeli naye Mungu akaona.

3 Naye Musa akawa mchungaji wa kundi la Yethro,[b] kuhani wa Midiani, aliyekuwa mwana-mkwe wake.[c] Alipokuwa akiliongoza kundi kuelekea upande wa magharibi wa nyika, mwishowe akafika kwenye mlima wa Mungu wa kweli,[d] Horebu.[e] **2** Ndipo malaika wa Yehova akamtokea katika mwali wa moto katikati ya mti wa miiba.[f] Alipoendelea kuangalia, tazama, ule mti wa miiba ulikuwa ukiwaka moto lakini haukuwa ukiteketea. **3** Ndipo Musa akasema: "Acha nigeuke nichunguze ajabu hii kubwa, kwa nini mti wa miiba hauteketei."[g] **4** Yehova alipoona kwamba alikuwa amegeuka achunguze, Mungu akamwita mara moja toka katikati ya ule mti wa miiba na kusema: "Musa! Musa!" naye akajibu: "Mimi hapa."[h] **5** Kisha akasema: "Usikaribie hapa. Vua viatu vyako kutoka miguuni, kwa sababu mahali ambapo umesimama ni udongo mtakatifu."[i]

6 Naye akaendelea kusema: "Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo."[j] Kisha Musa akauficha uso wake, kwa sababu aliogopa kumtazama Mungu wa kweli. **7** Naye Yehova akaongezea: "Pasipo shaka nimeyaona mateso ya watu wangu walio Misri, nami nimesikia kilio chao kwa sababu ya wale wanaowalazimisha kufanya kazi; kwa sababu nayajua vizuri maumivu waliyo nayo.[k] **8** Nami ninashuka ili kuwakomboa kutoka katika mkono wa Wamisri[l]

SURA 2

a Mwa 25:2
Kut 3:1
b Kut 18:12
c Mwa 24:20
d Mwa 29:10
e Kut 4:18
Kut 18:1
Hes 10:29
f Mdo 7:22
g Mwa 19:3
Mwa 24:31
Ayu 31:32
Ro 12:13
Ebr 13:2
h Kut 18:2
Hes 12:1
i Kut 18:3
1Nya 23:15
j Mdo 7:29
k Kut 4:19
Kut 7:7
Mdo 7:30
l Kut 6:5
Hes 20:16
Kum 26:7
Zb 12:5
m Kut 3:7
1Fa 8:51
Ne 9:9
Zb 107:19
n Amu 2:18
Ne 9:27
1Pe 5:7
o Mdo 7:34

Safu ya 2

a Mwa 15:14
2Fa 13:23
Zb 105:8

SURA 3

b Kut 2:16
Kut 18:1
c Amu 1:16
Amu 4:11
d Kut 24:13
e Kut 17:6
1Fa 19:8
Mal 4:4
f Kum 33:16
Mdo 7:30
g Mwa 18:14
Da 3:27
Mdo 7:31
h 1Sa 3:4
i Yos 5:15
Mdo 7:33
j Mwa 26:24
Mwa 32:9
Mt 22:32
Mdo 7:32
k Kut 1:11
Kut 6:5
Zb 106:44
Isa 63:9
Mdo 7:34
l Kut 12:51

na kuwatoa katika nchi hiyo mpaka kwenye nchi nzuri na kubwa, nchi inayotiririka maziwa na asali,[a] kwa Wakanaani na Wahiti na Waamori na Waperizi na Wahivi na Wayebusi.[b] **9** Na sasa, tazama! kilio cha wana wa Israeli kimenifikia, nami nimeona pia ukandamizaji ambao Wamisri wanatumia kuwakandamiza.[c] **10** Na sasa njoo, nikutume kwa Farao, nawe uwatoe watu wangu wana wa Israeli kutoka Misri."[d]

11 Hata hivyo, Musa akamwambia Mungu wa kweli: "Mimi ni nani hata niende kwa Farao, nikawatoe wana wa Israeli kutoka Misri?"[e] **12** Naye akajibu: "Kwa sababu nitakuwa pamoja nawe,[f] nayo hii ndiyo ishara kwako ya kwamba mimi ndiye niliyekutuma:[g] Baada ya kuwatoa watu hao Misri, ninyi mtamtumikia Mungu wa kweli kwenye mlima huu."[h]

13 Hata hivyo, Musa akamwambia Mungu wa kweli: "Tuseme nimefika kwa wana wa Israeli nami niwaambie, 'Mungu wa mababu zenu amenituma kwenu,' nao waniambie, 'Jina lake ni nani?'[i] Nitawaambia nini?" **14** Ndipo Mungu akamwambia Musa: "NITAKUWA KILE NITAKACHOKUWA."[j] Naye akaongeza kusema: "Hivi ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli, 'NITAKUWA amenituma kwenu.'"[k] **15** Kisha Mungu akamwambia Musa tena:

"Hivi ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli, 'Yehova Mungu wa mababu zenu, Mungu wa Abrahamu,[l] Mungu wa Isaka[m] na Mungu wa Yakobo,[n] amenituma kwenu.' Hilo ndilo jina langu mpaka wakati usio na kipimo,[o] na huo ndio ukumbusho wangu kwa kizazi baada ya kizazi.[a] **16** Wewe nenda, uwakusanye wanaume wazee wa Israeli, na kuwaambia, 'Yehova Mungu wa mababu zenu amenitokea,[b] Mungu wa Abrahamu, Isaka na Yakobo, na kusema: "Hakika nitaelekeza fikira[c] kwenu na kwa yale mnayotendewa katika Misri. **17** Na kwa hiyo nasema, Nitawatoa katika mateso[d] ya Wamisri na kuwapeleka mpaka nchi ya Wakanaani na Wahiti na Waamori[e] na Waperizi na Wahivi na Wayebusi,[f] mpaka nchi inayotiririka maziwa na asali."'[g]

18 "Nao hakika wataisikiliza sauti yako,[h] nawe utakuja, wewe pamoja na wanaume wazee wa Israeli, kwa Mfalme wa Misri, nanyi mtamwambia, 'Yehova Mungu wa Waebrania[i] amewasiliana nasi,[j] na sasa tunataka kwenda, tafadhali, safari ya siku tatu nyikani, nasi tunataka kumtolea dhabihu Yehova Mungu wetu.'[k] **19** Nami, naam, mimi najua vema kwamba mfalme wa Misri hatawapa ruhusa ya kwenda isipokuwa kupitia kwa mkono wenye nguvu.[l] **20** Nami nitaunyoosha mkono[m] wangu na kuipiga Misri kwa matendo yangu yote ya ajabu nitakayoyafanya katikati yake; kisha atawaruhusu mwondoke.[n] **21** Nami nitawapa watu hawa kibali machoni pa Wamisri; na hakika itakuwa kwamba mtakapoenda, hamtaenda mikono mitupu.[o] **22** Na kila mwanamke atamwomba jirani yake na mwanamke mgeni aliye katika nyumba yake, vyombo vya fedha na vyombo vya dhahabu na nguo za kujitanda, nanyi mtawatwika wana wenu na binti zenu; nanyi mtawaacha Wamisri bila chochote."[p]

SURA 3

a Hes 13:27
Kum 27:3
b Mwa 10:16
Kut 33:2
Kum 7:1
Yos 3:10
Ne 9:8
c Kut 1:11
d 1Sa 12:6
Zb 105:26
Isa 63:11
Mdo 7:34
e Kut 6:12
2Sa 7:18
Yer 1:6
f Kum 31:23
Yos 1:5
Isa 41:10
Ro 8:31
Flp 4:13
g Amu 6:17
h Kut 19:2
Kum 4:11
i Kut 15:3
1Sa 17:45
Zb 96:8
Zb 135:13
Ho 12:5
Mt 21:9
Yoh 17:26
Ro 10:13
j Law 11:45
Ayu 23:13
Isa 14:27
Da 4:35
Yoh 12:28
k Kut 6:3
Kut 6:7
Ro 9:17
l Mwa 17:7
Mt 22:32
m Mwa 26:24
n Mwa 28:13
o Zb 135:13

Safu ya 2

a Zb 30:4
Zb 102:12
Ho 12:5
b Mwa 17:1
Mwa 48:15
c Mwa 50:24
Kut 13:19
Zb 80:14
Lu 1:68
d Mwa 15:13
Law 26:13
Ne 9:9
Mdo 7:34
e Mwa 15:16
f Kut 23:23
g Hes 13:27
Kum 8:7
h Kut 4:31
Kut 20:19
i Mwa 14:13
Mwa 40:15
Kut 10:3
j Kut 5:3
k Kut 7:16
Kut 8:27
Kut 10:26
l Kut 5:2
Kut 7:4
Kut 14:8
Ro 9:17
m Zb 118:15
n Kut 7:3
Kut 12:33
Kum 6:22
Zb 135:9
Mdo 7:36
o Kut 11:2
Kut 12:35
p Mwa 15:14
Kut 12:36
Zb 105:37

4 Hata hivyo, Musa akajibu
na kusema: "Lakini tuseme
hawaniamini wala hawaisikilizi
sauti yangu,[a] kwa sababu wata-
sema, 'Yehova hakukutokea.'"
2 Ndipo Yehova akamwambia:
"Ni nini hicho kilicho mko-
noni mwako?" naye akajibu:
"Fimbo."[b] **3** Kisha akasema:
"Itupe chini." Basi akaitupa chi-
ni, nayo ikawa nyoka;[c] na Musa
akaanza kumkimbia. **4** Sasa
Yehova akamwambia Musa:
"Nyoosha mkono wako umka-
mate kwenye mkia." Basi akau-
nyoosha mkono wake, akamka-
mata, naye akawa fimbo mko-
noni mwake. **5** "Ili kwamba,"
kama alivyosema, "wapate ku-
amini ya kwamba Yehova Mu-
ngu wa mababu zao,[d] Mungu wa
Abrahamu,[e] Mungu wa Isaka[f]
na Mungu wa Yakobo,[g] ameku-
tokea."[h]
6 Kisha Yehova akamwa-
mbia tena: "Tia mkono wako,
tafadhali, ndani ya mkunjo wa
juu wa vazi lako." Basi akau-
tia mkono wake ndani ya mku-
njo huo. Alipouchomoa, tazama,
mkono wake ulikuwa ume-
patwa na ukoma kama theluji![i]
7 Kisha akasema: "Rudisha
mkono wako ndani ya mkunjo
wa juu wa vazi lako." Basi aka-
urudisha mkono wake ndani ya
mkunjo huo. Alipouchomoa ku-
toka katika mkunjo huo, ta-
zama, ulikuwa umerudishwa
ukawa kama sehemu nyingi-
ne ya mwili wake![j] **8** "Na ita-
kuwa kwamba," kama alivyo-
sema, "ikiwa hawatakuamini
wala kuisikiliza sauti ya ishara
ya kwanza, basi hakika wataia-
mini sauti ya ishara hiyo ya ba-
adaye.[k] **9** Hata hivyo, itaku-
wa kwamba, ikiwa hawatazi-
amini ishara hizo mbili wala
kuisikiliza sauti yako,[l] basi uta-
chukua maji kutoka katika Mto
Nile na kuyamwaga kwenye
nchi kavu; nayo maji utakayo-
chukua kutoka katika Mto Nile
hakika yatakuwa, ndiyo, kwa
kweli yatakuwa damu juu ya
nchi kavu."[a]
10 Ndipo Musa akamwambia
Yehova: "Nakuomba radhi, Ye-
hova, lakini mimi si msemaji
mzuri, tangu jana wala tangu
kabla ya hapo wala tangu ulipo-
sema na mtumishi wako, kwa
maana kinywa changu ni kizi-
to na ulimi wangu ni mzito."[b]
11 Ndipo Yehova akamwa-
mbia: "Ni nani aliyekifanya ki-
nywa kwa ajili ya mwanadam-
u au ni nani ambaye humfa-
nya mtu kuwa bubu au kizi-
wi au mwenye kuona vizuri
au kipofu? Je, si mimi, Yehova?[c]
12 Basi sasa, nenda, nami nita-
kuwa pamoja na kinywa cha-
ko nami nitakufundisha una-
yopaswa kusema."[d] **13** Laki-
ni akasema: "Nakuomba radhi,
Yehova, lakini tuma, tafadha-
li, kupitia mkono wa yule uta-
kayemtuma." **14** Ndipo hasi-
ra ya Yehova ikawaka juu ya
Musa naye akasema: "Je, Ha-
runi Mlawi si ndugu yako?[e]
Najua kwamba anaweza kuo-
ngea kwelikweli. Na tena, ta-
zama, yuko njiani akija ku-
kupokea. Atakapokuona, haki-
ka atashangilia moyoni mwa-
ke.[f] **15** Nawe utasema naye
na kuyaweka maneno hayo ki-
nywani mwake;[g] nami nitaku-
wa pamoja na kinywa chako na
kinywa chake,[h] nami nitawafu-
ndisha mambo mtakayofanya.[i]
16 Naye atasema na watu kwa
ajili yako; na itakuwa kwamba
yeye atatumikia akiwa kinywa
kwako,[j] nawe utatumikia uki-
wa Mungu kwake.[k] **17** Nayo
fimbo hii utaichukua mkononi

SURA 4
a Kut 2:14
Mdo 7:25
b Kut 8:5
Kut 17:5
Hes 20:11
c Kut 7:9
d 1Sa 2:27
Mdo 7:32
e Mdo 7:2
Ro 4:3
f Mwa 28:13
Mk 12:26
g Mwa 28:21
Lu 20:37
h Kut 3:16
Kut 4:31
Yer 31:3
i Hes 12:10
2Fa 5:27
j 2Fa 5:14
Mt 8:3
k Yoh 10:38
Mdo 7:36
l 2Th 3:2

Safu ya 2
a Kut 4:30
b Kut 6:12
Hes 12:3
Yer 1:6
Mdo 7:22
2Ko 11:6
c Zb 94:9
Isa 6:10
Lu 1:20
Mdo 13:11
d Zb 51:15
Zb 143:10
Isa 50:4
Mk 13:11
Lu 12:12
e Hes 26:59
f Mwa 33:4
Kut 4:27
Mdo 7:30
g Kut 4:28
Kut 7:1
h Yer 1:9
i Isa 54:13
1Ko 1:5
2Ko 3:5
j Kut 7:2
k Kut 7:1
Zb 82:6
Yoh 10:34

mwako ili uitumie kufanya zile
ishara.”[a]
18 Basi Musa akarudi kwa
Yethro baba-mkwe wake na ku-
mwambia:[b] “Nataka kwenda,
tafadhali, nirudi kwa ndugu za-
ngu walio Misri ili nione kama
wangali hai.”[c] Kwa hiyo Yethro
akamwambia Musa: “Nenda
kwa amani.”[d] **19** Kisha Yeho-
va akamwambia Musa huko Mi-
diani: “Nenda, rudi Misri, kwa
sababu watu wote waliokuwa
wakiiwinda nafsi yako wame-
kufa.”[e]
20 Ndipo Musa akamchukua
mke wake na wanawe na ku-
wapandisha juu ya punda, naye
akarudi katika nchi ya Misri.
Na zaidi, Musa akaichukua ile
fimbo ya Mungu wa kweli mko-
noni mwake.[f] **21** Naye Yeho-
va akamwambia Musa: “Ukisha
kwenda na kurudi Misri
hakikisha umefanya miujiza
yote ambayo nimeitia mkono-
ni mwako mbele ya Farao.[g]
Mimi nami, nitauacha moyo
wake uwe mkaidi;[h] naye hata-
waruhusu watu waende zao.[i]
22 Nawe utamwambia Farao,
‘Hivi ndivyo Yehova amesema:
“Israeli ni mwanangu, mzaliwa
wangu wa kwanza.[j] **23** Nami
nakuambia wewe: Mruhusu
mwanangu aende zake ili ani-
tumikie. Lakini iwapo utaka-
taa kumruhusu aende zake, ta-
zama, nitamuua mwana wako,
mzaliwa wako wa kwanza.”’”[k]
24 Sasa ikawa kwamba wa-
lipokuwa barabarani, maha-
li pa kulala,[l] Yehova akakuta-
na naye,[m] naye akawa akitafuta
njia ya kumuua.[n] **25** Mwi-
showe Sipora[o] akachukua jiwe
gumu na kukata govi[p] la mwa-
nawe, akalifanya liguse mi-
guu yake, na kusema: “Ni kwa
sababu wewe ni bwana-aru-
si wa damu kwangu.” **26** Basi
akamwachilia. Ndipo akasema:
“Bwana-arusi wa damu,” kwa
sababu ya tohara.
27 Kisha Yehova akamwa-
mbia Haruni: “Nenda ukaku-
tane na Musa nyikani.”[a] Basi
akaenda akakutana naye kati-
ka mlima wa Mungu wa kwe-
li,[b] akambusu. **28** Naye Musa
akamwambia Haruni maneno
yote ya Yehova, aliyekuwa ame-
mtuma,[c] na ishara zote ali-
zokuwa amemwamuru kufa-
nya.[d] **29** Kisha Musa na Ha-
runi wakaenda na kuwaku-
sanya wanaume wote wazee wa
wana wa Israeli.[e] **30** Ndipo
Haruni akasema maneno yote
ambayo Yehova alikuwa ame-
mwambia Musa,[f] naye akafa-
nya ishara[g] machoni pa watu.
31 Kwa hiyo watu wakaami-
ni.[h] Waliposikia kwamba Yeho-
va alikuwa amewaelekezea fi-
kira[i] wana wa Israeli na kwa-
mba alikuwa ameyaona mateso
yao,[j] ndipo wakainama na ku-
sujudu.[k]
5 Na baadaye Musa na Haru-
ni wakaingia ndani na ku-
mwambia Farao:[l] “Hivi ndivyo
Yehova Mungu wa Israeli ame-
sema, ‘Waruhusu watu wangu
waende zao, wakanifanyie she-
rehe nyikani.’”[m] **2** Lakini Fa-
rao akasema: “Yehova ni nani,[n]
hivi kwamba mimi niitii sauti
yake na kuwaruhusu Israeli wa-
ende zao?[o] Simjui Yehova hata
kidogo[p] na tena sitawaruhusu
Israeli waende zao.”[q] **3** Hata
hivyo, wakaendelea kusema:
“Mungu wa Waebrania amewa-
siliana nasi.[r] Tunataka kwenda,
tafadhali, safari ya siku tatu
nyikani na kumtolea dhabihu
Yehova Mungu wetu;[s] ikiwa

SURA 4

a Kut 7:19
b Kut 2:18
Kut 18:1
Hes 10:29
c Mwa 30:25
Mdo 7:30
d 1Sa 1:17
e Kut 2:15
f Kut 17:9
Hes 20:8
g Kut 7:9
h Kut 7:3
Kut 10:1
Kut 11:10
Kum 2:30
1Sa 6:6
Da 5:20
Ro 9:18
i Kut 7:22
Kut 8:15
j Kum 7:6
Kum 14:2
Yer 31:9
Ho 11:1
Ro 9:4
k Kut 12:29
Zb 105:36
Zb 135:8
l Mwa 42:27
Yer 9:2
m Hes 22:22
1Nya 21:16
n Mwa 17:14
o Kut 2:21
Kut 18:2
p Yos 5:2

Safu ya 2

a Kut 4:14
b Kut 3:1
Kut 20:18
Kut 24:16
1Fa 19:8
c Kut 4:15
Kut 7:1
d Kut 4:8
e Kut 3:16
Kut 24:1
f Kut 3:16
g Kut 4:3
Kut 4:6
Kut 4:9
h Kut 3:18
Kut 4:8
i Mwa 50:25
Kut 13:19
j Kut 1:14
Kut 3:7
Kum 26:6
k Mwa 43:28
2Nya 7:3
Ne 8:6

SURA 5

l Kut 7:1
Kut 7:10
Zb 119:46
m Kut 10:9
n Kut 7:5
Kut 9:16
1Sa 25:10
o 2Fa 18:35
Ayu 21:15
Ro 1:21
p 1Sa 2:12
Yoh 16:3
2Th 1:8
q Kut 3:19
Kut 7:3
r Kut 3:18
Ro 3:29
s Mwa 46:1
Kut 8:27

sivyo huenda akatupiga kwa tauni au kwa upanga."[a] **4** Ndipo mfalme wa Misri akawaambia: "Kwa nini, Musa na Haruni, mnawafanya watu waache kazi zao?[b] Nendeni mkabebe mizigo yenu!"[c] **5** Naye Farao akaendelea kusema: "Tazama! Watu wa nchi hii sasa ni wengi,[d] nanyi kwa kweli mnawaachisha kubeba mizigo."[e]

6 Siku hiyo, mara moja Farao akawaamuru wale waliokuwa wakiwalazimisha watu kufanya kazi na maofisa[f] wao, na kusema: **7** "Msikusanye nyasi ili kuwapa watu watengeneze matofali[g] kama hapo zamani. Acheni wao wenyewe waende kujikusanyia nyasi. **8** Tena, jumla ya matofali yanayohitajiwa waliyokuwa wakiyatengeneza hapo zamani, mtazidi kuwadai. Msiwapunguzie hata kidogo, kwa sababu wanalegea.[h] Ndiyo sababu wanalia, wakisema, 'Tunataka kwenda, tunataka kumtolea Mungu wetu dhabihu!'[i] **9** Utumishi na uwe mzito juu ya watu hao na wa ufanyie kazi, wala wasisikilize maneno ya uwongo."[j]

10 Basi wale waliokuwa wakiwalazimisha watu kufanya kazi[k] na maofisa wao wakatoka na kuwaambia watu: "Hivi ndivyo Farao amesema, 'Siwapi ninyi nyasi tena. **11** Ninyi wenyewe nendeni, jitafutieni nyasi, popote mtakapoipata, kwa sababu utumishi wenu hautapunguzwa hata kidogo.'"[l] **12** Kwa hiyo watu wakatawanyika kotekote nchini Misri ili kukusanya majani makavu kuwa nyasi. **13** Na wale waliokuwa wakiwalazimisha kufanya kazi wakawa wakiwahimiza,[m] wakisema: "Malizeni kazi zenu, kila mmoja kazi yake, siku baada ya siku, kama wakati ambapo nyasi ilikuwa ikipatikana."[a] **14** Baadaye maofisa[b] wa wana wa Israeli, ambao wasimamizi wa kazi wa Farao walikuwa wamewaweka juu yao, wakapigwa,[c] wakiambiwa: "Kwa nini hamkumaliza kazi yenu mliyoamriwa ya kutengeneza matofali[d] kama hapo zamani, jana na pia leo?"[e]

15 Basi maofisa[f] wa wana wa Israeli wakaingia ndani na kuanza kumlilia Farao, na kusema: "Kwa nini unawatendea hivi watumishi wako? **16** Watumishi wako hawapewi nyasi yoyote na bado wanatuambia, 'Tengenezeni matofali!' na tazama, watumishi wako wanapigwa, hali watu wako mwenyewe ndio wenye makosa."[g] **17** Lakini yeye akasema: "Mnalegea, mnalegea![h] Ndiyo sababu mnasema, 'Tunataka kwenda, tunataka kumtolea Yehova dhabihu.'[i] **18** Na sasa nendeni, mkafanye utumishi! Ingawa hamtapewa nyasi yoyote, bado mtatengeneza jumla ya matofali iliyowekwa."[j]

19 Ndipo maofisa wa wana wa Israeli wakajiona ya kwamba wamo katika hali mbaya iliposemwa:[k] "Msipunguze hata kidogo kiwango cha matofali yanayotengenezwa na mtu kwa siku."[l] **20** Kisha wakakutana na Musa na Haruni,[m] waliokuwa wamesimama hapo ili wakutane nao walipokuwa wakitoka kwa Farao. **21** Wakawaambia mara moja: "Yehova na awatazame ninyi na kuhukumu,[n] kwa kuwa mmetufanya tunuke vibaya[o] mbele ya Farao na mbele ya watumishi wake kwa kuutia upanga mkononi mwao watuue."[p] **22** Kisha Musa akamgeukia Yehova[q]

SURA 5

a Kum 28:21
2Fa 17:25
b Yer 38:4
Mdo 16:20
c Kut 1:11
Kut 2:11
d Kut 1:9
e Kut 6:6
f Kut 3:7
g Mwa 11:3
Kut 1:14
Nah 3:14
h Kut 5:17
i Kut 10:25
j 2Fa 18:20
Yer 43:2
k Kut 1:11
Kut 3:7
l 1Fa 12:10
Mhu 7:7
m Kut 3:9

Safu ya 2

a Kum 26:7
Mhu 4:1
b Kum 29:10
c Kut 2:11
Mdo 7:24
d Nah 3:14
e Mwa 15:13
f Hes 11:16
Yoh 18:12
g Zb 37:12
h Kut 5:8
i Kut 3:18
Kut 5:3
Kut 10:25
j Kut 1:14
k Kut 5:7
l Kut 5:8
m Kut 7:1
n Amu 11:27
1Sa 2:10
Isa 33:22
o Mwa 34:30
1Sa 13:4
1Nya 19:6
p Kut 6:9
Kut 17:3
q Kut 17:4
Yer 12:1

na kusema: “Yehova, kwa nini umesababisha uovu uwapate watu hawa?[a] Kwa nini umenituma mimi?[b] **23** Kwa maana tangu wakati nilipoenda mbele ya Farao ili kusema katika jina lako,[c] amewafanyia watu hawa uovu,[d] nawe hujawakomboa watu wako hata kidogo.”[e]

6 Basi Yehova akamwambia Musa: “Sasa utaona nitakayomtendea Farao,[f] maana kwa sababu ya mkono wenye nguvu atawaruhusu waende zao na kwa sababu ya mkono wenye nguvu atawafukuza watoke katika nchi yake.”[g]

2 Naye Mungu akaendelea kusema na Musa na kumwambia: “Mimi ni Yehova.[h] **3** Nami nilikuwa nikimtokea Abrahamu,[i] Isaka[j] na Yakobo[k] kama Mungu Mweza-Yote,[l] lakini kuhusu jina langu Yehova[m] sikujifanya nijulikane[n] kwao. **4** Na pia nilifanya agano pamoja nao niwape nchi ya Kanaani, nchi ya makao yao ya kigeni walimokaa wakiwa wageni.[o] **5** Nami, naam mimi, nimesikia kuugua kwa wana wa Israeli,[p] ambao Wamisri wanawatumikisha, nami ninalikumbuka agano langu.[q]

6 “Kwa hiyo waambie wana wa Israeli, ‘Mimi ni Yehova, nami hakika nitawatoa chini ya mizigo ya Wamisri na kuwakomboa kutoka katika utumwa wao,[r] nami kwa kweli nitawaokoa ninyi kwa mkono ulionyooshwa na kwa hukumu kubwa.[s] **7** Nami hakika nitawachukua kwangu muwe watu wangu,[t] nami kwa kweli nitakuwa Mungu kwenu;[u] nanyi hakika mtajua kwamba mimi ni Yehova Mungu wenu anayewatoa kutoka chini ya mizigo ya Misri.[a] **8** Nami hakika nitawaingiza katika nchi ambayo niliuinua mkono wangu katika kiapo[b] kwamba nitampa Abrahamu, Isaka na Yakobo; nami kwa kweli nitawapa ninyi iwe mali yenu.[c] Mimi ni Yehova.’”[d]

9 Baadaye Musa akawaambia wana wa Israeli maneno hayo, lakini hawakumsikiliza Musa kwa sababu ya kuvunjika moyo na kwa sababu ya utumwa mgumu.[e]

10 Ndipo Yehova akaongea na Musa, na kusema: **11** “Ingia ndani, mwambie Farao, mfalme wa Misri,[f] kwamba inampasa awaruhusu wana wa Israeli waondoke katika nchi yake.”[g] **12** Hata hivyo, Musa akasema mbele za Yehova, na kumwambia: “Tazama! Wana wa Israeli hawakunisikiliza;[h] Farao atawezaje kunisikiliza,[i] kwa maana mimi sijatahiriwa midomo?”[j] **13** Lakini Yehova akaendelea kusema na Musa na Haruni na kuitoa amri kupitia kwao kwa wana wa Israeli na kwa Farao, mfalme wa Misri, ili kuwatoa wana wa Israeli kutoka katika nchi ya Misri.[k]

14 Hawa ndio vichwa vya nyumba za baba zao: Wana wa Rubeni, mzaliwa wa kwanza wa Israeli,[l] walikuwa Hanoki na Palu, Hezroni na Karmi.[m] Hizo ndizo familia za Rubeni.[n]

15 Nao wana wa Simeoni walikuwa Yemueli na Yamini na Ohadi na Yakini na Zohari na Shauli mwana wa mwanamke Mkanaani.[o] Hizo ndizo familia za Simeoni.[p]

16 Na haya ndiyo majina ya wana wa Lawi,[q] kulingana na

SURA 5

a Hes 11:11
1Sa 30:6
b Kut 3:12
c Kut 5:1
d Kut 5:9
e Kut 3:8

SURA 6

f Kut 12:29
Kut 14:13
Zb 12:5
g Kut 9:3
Kut 11:1
Kut 12:31
h Isa 43:11
i Mwa 18:1
j Mwa 26:2
k Mwa 28:13
l Mwa 17:1
Mwa 35:11
m Kut 10:2
Zb 83:18
Lu 11:2
Yoh 12:28
Mdo 15:14
Ufu 15:3
n Mwa 12:8
Mwa 27:27
Mwa 28:16
2Sa 7:23
Zb 9:16
Isa 52:6
Yer 16:21
Yer 32:20
o Mwa 15:18
Mwa 28:4
p Kut 2:24
q Mwa 17:7
r Kum 4:20
s Kut 7:5
Kum 26:8
1Nya 17:21
Mdo 13:17
t Kum 7:6
2Sa 7:24
Zb 33:12
u Kut 29:45
Kum 20:4

Safu ya 2

a Kut 1:14
Kut 7:5
Kut 9:16
Ro 9:17
b Ebr 6:13
c Mwa 15:18
Mwa 26:3
Mwa 35:12
Kut 32:13
d Kut 20:2
Isa 42:8
e Kut 5:21
f Kut 1:8
g Kut 3:10
Kut 5:1
h Kut 5:21
Kut 6:9
i Kut 5:2
j Kut 4:10
Yer 1:6
Mdo 7:22
k Kut 7:4
Kut 9:13
l Mwa 49:3
m Mwa 46:9
n Hes 26:7
Yos 13:15
o 1Nya 4:24
p Hes 26:14
Yos 21:9
q Mwa 29:34
1Nya 6:1

ukoo wa familia yao:[a] Gershoni na Kohathi na Merari.[b] Nayo miaka ya maisha ya Lawi ilikuwa miaka 137.

17 Wana wa Gershoni walikuwa Libni na Shimei,[c] kulingana na familia zao.[d]

18 Na wana wa Kohathi walikuwa Amramu na Ishari na Hebroni na Uzieli.[e] Nayo miaka ya maisha ya Kohathi ilikuwa miaka 133.

19 Na wana wa Merari walikuwa Mali na Mushi.[f]

Hizo ndizo zilizokuwa familia za Walawi, kulingana na ukoo wa familia yao.[g]

20 Sasa Amramu alimchukua Yokebedi dada ya baba yake awe mke wake.[h] Baadaye akamzalia Haruni na Musa.[i] Nayo miaka ya maisha ya Amramu ilikuwa miaka 137.

21 Na wana wa Ishari walikuwa Kora[j] na Nefegi na Zikri.

22 Na wana wa Uzieli walikuwa Mishaeli na Elsafani na Sithri.[k]

23 Sasa Haruni alimchukua Elisheba, binti ya Aminadabu, dada ya Nashoni,[l] awe mke wake. Baadaye akamzalia Nadabu na Abihu, Eleazari na Ithamari.[m]

24 Na wana wa Kora walikuwa Asiri na Elkana na Abiasafu.[n] Hizo ndizo zilizokuwa familia za Wakora.[o]

25 Na Eleazari, mwana wa Haruni,[p] alijichukulia mmoja wa binti za Putieli awe mke wake. Baadaye akamzalia Finehasi.[q]

Hao ndio vichwa vya upande wa baba vya Walawi, kulingana na familia zao.[r]

26 Huyo ndiye Haruni na Musa ambao Yehova aliwaambia:[s] "Watoeni wana wa Israeli kutoka katika nchi ya Misri kulingana na majeshi yao."[a] **27** Wao ndio waliokuwa wakisema na Farao, mfalme wa Misri, ili kuwatoa wana wa Israeli kutoka Misri.[b] Huyo ndiye Musa na Haruni.

28 Na ikawa siku ambayo Yehova alisema na Musa katika nchi ya Misri,[c] **29** kwamba Yehova aliongea na Musa, na kusema: "Mimi ni Yehova.[d] Mwambie Farao mfalme wa Misri kila jambo ninalokuambia." **30** Kisha Musa akasema mbele za Yehova: "Tazama! Mimi sijatahiriwa midomo, basi Farao atawezaje kunisikiliza mimi?"[e]

7 Kwa hiyo Yehova akamwambia Musa: "Tazama, nimekufanya wewe kuwa Mungu kwa Farao,[f] na Haruni ndugu yako atakuwa nabii wako.[g] **2** Wewe—wewe utasema mambo yote nitakayokuamuru;[h] naye Haruni ndugu yako atamwambia Farao,[i] naye lazima awaruhusu wana wa Israeli waondoke nchini mwake.[j] **3** Mimi nami, nitauacha moyo wa Farao uwe mkaidi,[k] nami hakika nitazidisha ishara zangu na miujiza yangu katika nchi ya Misri.[l] **4** Na Farao hatawasikiliza ninyi;[m] nami nitalazimika kuuweka mkono wangu juu ya Misri na kuleta majeshi yangu,[n] watu wangu,[o] wana wa Israeli,[p] kutoka katika nchi ya Misri kwa hukumu kubwa.[q] **5** Na Wamisri hakika watajua kwamba mimi ni Yehova wakati ambapo nitaunyoosha mkono wangu juu ya Misri,[r] nami kwa kweli nitawatoa wana wa Israeli kutoka katikati yao."[s] **6** Na Musa na Haruni wakafanya kama vile Yehova alivyokuwa amewaamuru.[t]

SURA 6

a Hes 26:57
b Mwa 46:11
c 1Nya 23:7
d Hes 3:18
e Hes 3:19
1Nya 23:12
f Hes 3:20
1Nya 23:21
g Yos 21:40
1Nya 6:19
h Kut 2:1
Hes 26:59
i 1Nya 23:13
j Hes 16:1
Hes 16:32
Hes 26:10
k Law 10:4
Hes 3:30
l Ru 4:20
Mt 1:4
m Hes 3:2
n Hes 26:11
1Nya 6:37
o Hes 26:58
1Nya 9:19
p Hes 3:32
q Hes 25:7
Hes 31:6
Yos 22:31
Amu 20:28
r Kut 6:19
s Yos 24:5
1Sa 12:6

Safu ya 2

a Kut 7:4
Kut 12:41
Mdo 7:35
b Kut 33:1
Zb 77:20
Mik 6:4
c Kut 6:1
d Kut 6:2
e Kut 4:10
Kut 6:12

SURA 7

f Kut 4:16
Zb 82:6
g Kut 4:15
Kut 4:30
h Kut 4:12
i Kut 4:15
j Kut 6:11
k Kut 4:21
Kut 8:15
Kut 9:12
Ro 9:18
l Kut 3:20
Kut 11:9
Zb 105:27
Mdo 7:36
m Kut 9:35
n Kut 12:51
o Kut 5:1
p Kut 6:11
q Kut 6:6
Kut 12:12
r Kut 3:19
Kut 8:19
Kut 8:22
Kut 14:4
Zb 83:18
s Kut 3:20
t Kut 4:28

Walifanya vivyo hivyo.[a] **7** Na
Musa alikuwa na umri wa mia-
ka 80 naye Haruni alikuwa na
umri wa miaka 83 wakati wali-
posema na Farao.[b]
8 Sasa Yehova akamwambia
Musa na Haruni: **9** "Ikiwa Fa-
rao atanena nanyi, na kusema,
'Jifanyieni muujiza,'[c] basi uta-
mwambia Haruni, 'Chukua fi-
mbo yako,[d] uitupe chini mbele
ya Farao.' Itakuwa nyoka mku-
bwa."[e] **10** Kwa hiyo Musa na
Haruni wakaingia ndani kwa
Farao na kufanya sawasawa
na vile ambavyo Yehova ali-
kuwa ameamuru. Basi Haruni
akaitupa chini fimbo yake mbe-
le ya Farao na watumishi wake
nayo ikawa nyoka mkubwa.
11 Hata hivyo, Farao pia ali-
waita watu wenye hekima na
walozi;[f] na makuhani wa Mi-
sri wenye kufanya uchawi nao
pia wakafanya jambo hilo hilo
kwa ufundi wao wa uchawi.[g]
12 Kwa hiyo kila mmoja wao
akatupa chini fimbo yake, nazo
zikawa nyoka wakubwa; lakini
fimbo ya Haruni ikameza fimbo
zao. **13** Bado, moyo wa Farao
ukawa mkaidi,[h] naye hakuwa-
sikiliza, kama Yehova alivyoku-
wa amesema.
14 Ndipo Yehova akamwa-
mbia Musa: "Moyo wa Farao ni
mgumu.[i] Amekataa kuwaruhu-
su watu waende zao.[j] **15** Ne-
nda kwa Farao asubuhi. Taza-
ma! Anaenda majini![k] Nawe usi-
mame mahali ili kukutana naye
kwenye ukingo wa Mto Nile,[l]
nayo fimbo iliyogeuka na kuwa
nyoka uichukue mkononi mwa-
ko.[m] **16** Nawe utamwambia,
'Yehova Mungu wa Waebra-
nia amenituma kwako,[n] na ku-
sema: "Waruhusu watu wangu
waende zao wakanitumikie nyi-
kani,"[o] lakini, tazama, wewe
hujatii mpaka sasa. **17** Hivi
ndivyo Yehova amesema:[a] "Kwa
hili utajua kwamba mimi ni
Yehova.[b] Tazama, ninayapiga
maji yaliyo katika Mto Nile[c]
kwa fimbo niliyo nayo mkono-
ni, nayo hakika yatageuka na
kuwa damu.[d] **18** Na samaki
walio katika Mto Nile watakufa,[e]
nao Mto Nile utanuka kwe-
likweli,[f] nao Wamisri hawata-
kuwa na hamu hata kidogo
ya kunywa maji kutoka katika
Mto Nile.""[g]
19 Baadaye Yehova akamwa-
mbia Musa: "Mwambie Haru-
ni, 'Ichukue fimbo yako na ku-
unyoosha mkono[h] wako juu ya
maji ya Misri, juu ya mito yao,
juu ya mifereji yao ya Nile na
juu ya madimbwi yao yenye ma-
tete[i] na juu ya maji yao yote
yaliyozuiliwa, ili yawe damu.'
Na hakika damu itakuwa kati-
ka nchi yote ya Misri na kati-
ka vyombo vya mbao na kati-
ka vyombo vya mawe."
20 Musa na Haruni wakafa-
nya hivyo mara moja,[j] kama
vile Yehova alivyokuwa ame-
amuru,[k] naye akainua fimbo
na kuyapiga maji ya Mto Nile
machoni pa Farao na watumi-
shi wake,[l] nayo maji yote yali-
yokuwa katika Mto Nile yaka-
geuzwa kuwa damu.[m] **21** Na
samaki waliokuwa katika Mto
Nile wakafa,[n] nao Mto Nile uka-
anza kunuka; nao Wamisri ha-
wakuweza kunywa maji kuto-
ka katika Mto Nile;[o] na damu
ikawa katika nchi yote ya Misri.
22 Hata hivyo, makuhani
wa Misri wenye kufanya
uchawi wakafanya jambo hilo
hilo kwa ufundi wao wa siri;[p]
hivi kwamba moyo wa Farao
ukaendelea kuwa mkaidi,[q] naye
hakuwasikiliza, kama vile Ye-
hova alivyokuwa amesema.[r]

SURA 7
a Mwa 6:22
Kut 12:28
b Kum 34:7
Mdo 7:23
c Isa 7:11
Mt 12:39
Yoh 6:30
d Kut 4:2
Kut 9:23
e Kut 4:3
f Mwa 41:8
Isa 19:11
Yer 27:9
Da 2:2
2Ti 3:8
Ufu 21:8
g Kut 7:22
Kut 8:18
Kut 9:11
Mdo 8:9
2Th 2:9
h Kut 4:21
Kut 7:3
Kut 8:15
Ro 9:18
i Kut 10:1
1Sa 6:6
j Kut 10:20
k Kut 2:5
Kut 8:20
l Kut 9:13
m Kut 4:3
n Kut 3:18
Kut 9:1
Ro 3:29
o Kut 5:1

Safu ya 2
a 1Fa 20:28
b Kut 7:5
Kut 8:22
Eze 25:17
c Kut 4:9
d Zb 78:44
e Zb 105:29
f Isa 50:2
g Kut 7:24
h Kut 9:22
Kut 10:12
Kut 14:21
i Kut 8:5
j Kut 7:6
Kut 12:28
k Kut 4:28
l Kut 17:5
m Zb 78:44
n Zb 105:29
o Kut 7:18
Kut 7:24
p Kut 7:11
Kut 8:7
Da 1:20
Mdo 8:9
2Ko 11:14
2Ti 3:8
q Kut 4:21
Kut 8:15
Ro 9:18
r Kut 3:19

23 Basi Farao akageuka na
kuingia nyumbani mwake,
naye hakuuruhusu moyo wake
ufikirie jambo hilo kwa uzi-
to.[a] **24** Na Wamisri wote wa-
kaanza kuchimba kuuzunguka
Mto Nile wakitafuta maji ya
kunywa, kwa sababu hawaku-
weza kunywa maji yoyote ya
Mto Nile.[b] **25** Na siku saba zi-
katimia baada ya Yehova kuupi-
ga Mto Nile.

8 Kisha Yehova akamwambia
Musa: "Ingia kwa Farao,
nawe umwambie, 'Hivi ndivyo
Yehova amesema: "Waruhusu
watu wangu waende zao ili wa-
nitumikie.[c] **2** Na ikiwa uta-
endelea kukataa kuwaruhu-
su waende zao, tazama, nitale-
ta pigo la vyura[d] katika eneo
lako lote. **3** Nao Mto Nile utaja-
a vyura, nao hakika watapa-
nda na kuingia ndani ya nyu-
mba yako na ndani ya chu-
mba chako cha ndani cha kula-
la na juu ya kitanda chako na
ndani ya nyumba za watumishi
wako na juu ya watu wako na
ndani ya majiko yako na ndani
ya vyombo vyako vya kukandia
unga.[e] **4** Na vyura hao wata-
kuja juu yako na juu ya watu
wako na juu ya watumishi wako
wote."'"[f]
5 Baadaye Yehova akamwa-
mbia Musa: "Mwambie Haruni,
'Nyoosha mkono wako pamoja
na fimbo[g] yako juu ya mito, mi-
fereji ya Nile na madimbwi ye-
nye matete na kuwafanya vyu-
ra waje juu ya nchi ya Misri.'"
6 Ndipo Haruni akaunyoosha
mkono wake juu ya maji ya Mi-
sri, na vyura wakaanza kuja
juu na kuifunika nchi ya Mi-
sri. **7** Hata hivyo, makuhani
wenye kufanya uchawi wakafa-
nya jambo hilo hilo kwa ufundi
wao wa siri na kuwafanya vyu-
ra waje juu ya nchi ya Misri.[a]
8 Mwishowe Farao akawaita
Musa na Haruni na kusema:
"Msihi Yehova[b] ili awaondoe
vyura hawa kutoka kwangu na
kwa watu wangu, kwa maana
nataka kuwaruhusu watu wa-
ende zao, wakamtolee Yeho-
va dhabihu."[c] **9** Kisha Musa
akamwambia Farao: "Jitwalie
utukufu kutoka kwangu na ku-
sema ni wakati gani nitakaposi-
hi kwa ajili yako na watumishi
wako na watu wako ili kuwa-
ondolea mbali hao vyura kuto-
ka kwenu na nyumbani mwenu.
Watabaki katika Mto Nile tu."
10 Naye akajibu: "Kesho." Basi
akasema: "Itakuwa kulingana
na neno lako, ili ujue kwamba
hakuna mwingine yeyote ali-
ye kama Yehova Mungu wetu,[d]
11 kwa kuwa hakika vyura wa-
taondoka kwako na nyumbani
mwako na kuondoka kwa watu-
mishi wako na watu wako. Wa-
tabaki katika Mto Nile tu."[e]
12 Basi Musa na Haruni wa-
kaondoka kwa Farao, naye
Musa akamlilia Yehova[f] kwa sa-
babu ya vyura hao ambao Yeye
alikuwa ameweka juu ya Farao.
13 Kisha Yehova akafanya ku-
lingana na neno la Musa,[g] na
vyura wakaanza kufa kutoka
katika nyumba, nyua na ma-
shamba. **14** Nao wakawaku-
sanya, mafungu mafungu, nayo
nchi ikaanza kunuka.[h] **15** Far-
ao alipoona kwamba kituli-
zo kilikuwa kimetokea, akaufa-
nya moyo wake uwe mgumu;[i]
naye hakuwasikiliza wao, kama
vile Yehova alivyokuwa ame-
sema.[j]
16 Sasa Yehova akamwambia
Musa: "Mwambie Haruni, 'Inyo-
oshe fimbo[k] yako na kuyapiga
mavumbi ya dunia, nayo yata-

SURA 7
a Kut 9:21
Met 29:1
Yer 5:3
b Kut 7:18

SURA 8
c Kut 3:12
Kut 5:1
d Kut 12:12
Yos 24:5
Zb 78:45
e Kut 12:34
Zb 105:30
f Da 4:37
g Kut 4:20
Kut 17:9

Safu ya 2
a Kut 7:11
Kut 7:22
Kut 8:18
2Ti 3:8
b Mwa 20:7
Kut 10:17
Hes 21:7
1Fa 13:6
Mdo 8:24
c Kut 8:15
Kut 8:29
Kut 10:8
Kut 12:31
d Kut 9:14
Kut 15:11
2Sa 7:22
Zb 83:18
Zb 86:8
Isa 46:9
Yer 10:6
Ro 9:17
e Kut 8:3
f Kut 8:30
Kut 9:33
Yak 5:16
g Kum 34:10
h Kut 7:21
i Kut 4:21
Kut 7:3
Met 21:29
Ro 9:18
j Isa 26:10
Yer 34:11
k Kut 17:9

kuwa chawa katika nchi yote ya
Misri.'" **17** Nao wakafanya hi-
vyo. Kwa hiyo Haruni akaunyo-
osha mkono wake pamoja na fi-
mbo yake na kuyapiga mavumbi
ya dunia, nao chawa wakawa
juu ya wanadamu na wanyama.
Mavumbi yote ya dunia yakawa
chawa katika nchi yote ya Mi-
siri.[a] **18** Nao makuhani wenye
kufanya uchawi wakajaribu ku-
fanya vivyo hivyo kwa ufundi
wao wa siri,[b] ili kutokeza chawa,
lakini hawakuweza.[c] Na chawa
hao wakawa juu ya wanadamu
na wanyama. **19** Basi makuha-
ni wenye kufanya uchawi waka-
mwambia Farao: "Ni kidole[d] cha
Mungu!"[e] Lakini moyo wa Farao
ukaendelea kuwa mkaidi,[f] naye
hakuwasikiliza, kama vile Yeho-
va alivyokuwa amesema.

20 Kisha Yehova akamwa-
mbia Musa: "Amka asubuhi na
mapema usimame mbele ya
Farao.[g] Tazama! Anatoka kwe-
nda majini! Nawe utamwambia,
'Hivi ndivyo Yehova amesema:
"Waruhusu watu wangu waende
zao ili wanitumikie.[h] **21** Laki-
ni ikiwa hutawaruhusu watu wa-
ngu waende zao, tazama, nita-
tuma mainzi[i] juu yako na wa-
tumishi wako na watu wako
na ndani ya nyumba zako; nazo
nyumba za Wamisri zitajaa mai-
nzi, na pia nchi ambayo wako
juu yake. **22** Na siku hiyo ha-
kika nitaifanya nchi ya Goshe-
ni ambapo watu wangu wanakaa
iwe tofauti, kwamba inzi yeyote
asiwe huko;[j] ili upate kujua kwa-
mba mimi ni Yehova katikati
ya dunia.[k] **23** Nami kwa kwe-
li nitaweka mpaka kati ya watu
wangu na watu wako.[l] Kesho
ishara hii itatokea.""

24 Naye Yehova akafanya
hivyo; na makundi makubwa
ya mainzi yakaanza kuvamia
nyumba ya Farao na nyumba
za watumishi wake na nchi
yote ya Misri.[a] Nchi ikaharibi-
ka kwa sababu ya mainzi hao.[b]
25 Mwishowe Farao akawaita
Musa na Haruni na kusema:
"Nendeni, mtoleeni Mungu
wenu dhabihu nchini."[c]
26 Lakini Musa akasema: "Ha-
ikubaliki kufanya hivyo, kwa
sababu tutamtolea Yehova Mu-
ngu wetu dhabihu ya kitu
ambacho ni chukizo kwa Wami-
siri.[d] Tuseme tungetoa dhabihu
ya kitu ambacho ni chukizo ma-
choni pa Wamisri; je, hawange-
tupiga kwa mawe? **27** Tutae-
nda safari ya siku tatu nyikani
nasi hakika tutamtolea Yehova
Mungu wetu dhabihu sawasawa
na alivyotuambia."[e]

28 Farao sasa akasema:
"Mimi—mimi nitawaruhusu
mwende zenu,[f] nanyi kwa kweli
mtamtolea dhabihu Yehova Mu-
ngu wenu nyikani.[g] Ila tu msie-
nde mbali sana. Sihi kwa ajili ya-
ngu."[h] **29** Ndipo Musa akase-
ma: "Tazama, naondoka kwako,
nami kwa kweli nitamsihi Ye-
hova, na hakika mainzi wataon-
doka kwa Farao, kwa watumi-
shi wake na kwa watu wake ke-
sho. Ila Farao asifanye mchezo
tena kwa kukataa kuwaruhu-
su watu waende zao kumto-
lea Yehova dhabihu."[i] **30** Ki-
sha Musa akaondoka mbele ya
Farao na kumsihi Yehova.[j]
31 Basi Yehova akafanya
kulingana na neno la Musa,[k] na
mainzi wakaondoka kwa Farao,
kwa watumishi wake na kwa
watu wake.[l] Hakuna hata mmoja
aliyebaki. **32** Hata hivyo, Fa-
rao akaufanya moyo wake uwe
mgumu wakati huu pia wala ha-
kuwaruhusu watu waende zao.[m]

SURA 8

a Zb 105:31
b Kut 7:11
Kut 9:11
Da 1:20
2Ti 3:8
c Mwa 41:8
Da 2:10
d Kut 31:18
Mt 12:28
Lu 11:20
e Kut 12:12
f Kut 14:8
Kum 2:30
Yos 11:20
1Sa 6:6
g Kut 7:15
h Kut 8:1
i Zb 78:45
Zb 105:31
j Kut 9:4
Kut 10:23
Kut 11:7
Kut 12:13
k Kut 7:5
Kut 8:10
1Sa 17:46
1Fa 20:28
2Fa 19:19
Eze 34:30
l Mal 3:18

Safu ya 2

a Kut 8:3
b Zb 78:45
Zb 105:31
c Kut 5:2
Kut 7:2
d Mwa 43:32
Mwa 46:34
Kut 10:26
e Mwa 8:20
Kut 3:12
Kut 3:18
Kut 5:3
f Kut 9:28
g Kut 7:16
h Kut 8:8
Kut 9:28
1Sa 12:19
Mdo 8:24
i Kut 8:8
Kut 8:15
Zb 78:36
Ga 6:7
j Kut 9:33
Yak 5:16
k Zb 65:2
l 1Fa 13:6
m Kut 4:21
Met 28:14
Mdo 28:27
Ro 2:5
Ro 9:18

9 Kwa hiyo Yehova akamwambia Musa: "Ingia ndani kwa Farao, umwambie,[a] 'Hivi ndivyo Yehova Mungu wa Waebrania amesema: "Waruhusu watu wangu waende zao wapate kunitumikia. **2** Lakini ukiendelea kukataa kuwaruhusu waende zao nawe ukiendelea kuwazuia,[b] **3** tazama! mkono wa Yehova[c] utakuja juu ya mifugo[d] yako iliyo shambani. Kutakuwa na tauni kali sana[e] juu ya farasi, punda, ngamia, mifugo na makundi. **4** Na Yehova hakika atafanya tofauti kati ya mifugo ya Israeli na mifugo ya Misri, wala hakuna chochote cha wana wa Israeli kitakachokufa."'"[f] **5** Tena, Yehova akaweka wakati, na kusema: "Kesho Yehova atafanya jambo hilo katika nchi."[g]

6 Basi Yehova akafanya jambo hilo siku iliyofuata, na aina zote za mifugo ya Wamisri zikaanza kufa;[h] lakini hakuna mnyama yeyote kati ya mifugo ya wana wa Israeli aliyekufa. **7** Kisha Farao akatuma watu, na, tazama! hakuna hata mnyama mmoja kati ya mifugo ya Israeli aliyekuwa amekufa. Hata hivyo, moyo wa Farao ukaendelea kuwa mgumu,[i] naye hakuwaruhusu watu waende zao.

8 Kisha Yehova akawaambia Musa na Haruni: "Chukueni masizi kutoka katika tanuru,[j] yaliyojaa kwenye mikono yote miwili, naye Musa ayarushe kuelekea mbinguni mbele ya macho ya Farao. **9** Nayo yatakuwa mavumbi juu ya nchi yote ya Misri, nayo yatakuwa majipu yanayopasuka na yenye malengelenge[k] juu ya mwanadamu na mnyama katika nchi yote ya Misri."

SURA 9

a Kut 5:1
Kut 8:1
b Kut 4:23
Kut 8:2
Zb 68:21
Met 6:15
c Kut 7:4
Kut 8:19
1Sa 5:7
Zb 39:10
Mdo 13:11
d Zb 78:48
e Kut 9:15
Zb 78:50
Eze 14:21
Amo 4:10
f Kut 8:22
Kut 10:23
Kut 11:7
Kut 12:13
Isa 65:13
Mal 3:18
g Kut 8:23
Zb 76:12
h Zb 78:48
i Kut 4:21
1Sa 6:6
Ayu 9:4
Met 29:1
Da 5:20
Ro 9:18
j Mwa 11:3
Mwa 19:28
k Law 13:18
Kum 28:35
Ayu 2:7

Safu ya 2

a Kum 28:27
b Kut 7:11
Kut 8:18
2Ti 3:8
c Kut 4:21
Kut 8:32
Kut 14:17
Yos 11:20
2Nya 36:13
Zb 75:5
d Kut 7:15
e Kut 7:16
f Kut 8:10
Kum 33:26
2Sa 7:22
Zb 71:19
Zb 83:18
Isa 45:5
Isa 46:9
Yer 10:7
g Kut 3:20
Kut 9:3
h Kut 14:17
Met 16:4
i Yos 2:10
1Nya 16:24
Isa 63:12
Mal 1:11
Ro 9:17
j Ayu 9:4
Isa 37:23

10 Basi wakachukua masizi ya tanuru na kusimama mbele ya Farao, naye Musa akayarusha kuelekea mbinguni, nayo yakawa majipu yenye malengelenge,[a] yanayopasuka juu ya mwanadamu na mnyama. **11** Nao makuhani wenye kufanya uchawi hawakuweza kusimama mbele ya Musa kutokana na majipu, kwa sababu makuhani hao na Wamisri wote walikuwa wamepata majipu hayo.[b] **12** Lakini Yehova akauacha moyo wa Farao uwe mkaidi, naye hakuwasikiliza, kama vile Yehova alivyokuwa amemwambia Musa.[c]

13 Kisha Yehova akamwambia Musa: "Amka asubuhi na mapema usimame mbele ya Farao,[d] nawe umwambie, 'Hivi ndivyo Yehova Mungu wa Waebrania amesema: "Waruhusu watu wangu waende zao wapate kunitumikia.[e] **14** Kwa maana wakati huu ninatuma mapigo yangu yote juu ya moyo wako na juu ya watumishi wako na watu wako, ili upate kujua kwamba hakuna yeyote aliye kama mimi katika dunia yote.[f] **15** Kwa maana kufikia sasa ningalikuwa nimenyoosha mkono wangu nipate kukupiga wewe na watu wako kwa tauni ili ufutiliwe mbali kutoka duniani.[g] **16** Lakini, kwa kweli, kwa sababu hii nimekuacha uendelee kuwako,[h] ili kukuonyesha nguvu zangu na ili nifanye jina langu litangazwe katika dunia yote.[i] **17** Je, bado unajiendesha kwa majivuno juu ya watu wangu kwa kutowaruhusu waende zao?[j] **18** Tazama, kesho wakati kama huu nitafanya mvua kubwa sana ya mawe inyeshe, mvua

ambayo haijapata kunyesha
Misri tangu siku ilipowekwa
msingi mpaka sasa.[a] **19** Na
sasa tuma watu, uingize mifu-
go yako yote na vitu vyote vili-
vyo vyako shambani mahali pa
kujikinga. Na kuhusu mwana-
damu na mnyama yeyote ataka-
yepatikana shambani, bila ku-
ingia nyumbani, mvua hiyo ya
mawe[b] itawaangukia, nao wata-
kufa.""
20 Yeyote aliyeogopa neno
la Yehova kati ya watumishi wa
Farao aliwakimbiza watumishi
wake na mifugo wake ndani
ya nyumba,[c] **21** lakini yeyote
ambaye moyo wake haukujali
neno la Yehova aliwaacha watu-
mishi wake na mifugo yake sha-
mbani.[d]
22 Sasa Yehova akamwa-
mbia Musa: "Nyoosha mkono[e]
wako kuelekea mbinguni, ili
mvua ya mawe[f] ipate kunyesha
juu ya nchi yote ya Misri, juu
ya mwanadamu na mnyama na
mimea yote ya shambani katika
nchi ya Misri." **23** Kwa hiyo
Musa akainyoosha fimbo yake
kuelekea mbinguni; na Yeho-
va akatoa mingurumo na
mvua ya mawe,[g] na moto
ulikuwa ukishuka chini mpa-
ka duniani, naye Yehova aka-
fanya mvua ya mawe iendelee
kunyesha juu ya nchi ya Misri.
24 Basi mvua ya mawe ikanye-
sha, nao moto ukiwaka-waka
katikati ya mvua ya mawe. Ili-
kuwa nzito sana, hivi kwa-
mba haikuwa imetokea yoyo-
te kama hiyo katika nchi yote
ya Misri tangu ilipokuwa taifa.[h]
25 Nayo mvua ya mawe ikapi-
ga nchi yote ya Misri. Mvua
ya mawe ikapiga kila kitu kili-
chokuwa shambani, kuanzia
mwanadamu mpaka mnyama,
na kila aina ya mimea ya sha-

SURA 9

a Zb 78:47
Zb 105:32

b Yos 10:11

c Met 22:3
Yon 3:5

d Kut 7:23

e Kut 7:19
Kut 8:5

f Kut 10:5
Ayu 38:22
Zb 78:47
Zb 105:32

g Zb 148:8
Isa 30:30

h Kut 9:18

Safu ya 2

a Zb 105:33

b Kut 8:22
Kut 9:4

c 1Sa 26:21
Zb 12:2
Mt 27:4

d Zb 129:4
Zb 145:17
Da 9:14
Ro 2:5

e Kut 8:8
Kut 10:17
Mdo 8:24

f 1Fa 8:22
Ezr 9:5
Zb 143:6

g Kum 10:14
Zb 24:1
Zb 50:12
1Ko 10:26

h Met 16:6
Isa 26:10
Lu 16:31

i Ru 1:22

j Isa 28:25
Eze 4:9

k Kut 10:18
Yak 5:17

l Kut 4:21
Kut 8:15
Kum 2:30
Yos 11:20
Ro 9:18

mbani; nayo ikavunja-vunja na-
mna zote za miti ya shambani.[a]
26 Ila tu katika nchi ya Goshe-
ni, ambako wana wa Israeli wa-
likuwa, hakukuwa na mvua yo-
yote ya mawe.[b]
27 Mwishowe Farao akawa-
tuma watu wawaite Musa na
Haruni, naye akawaambia: "Ni-
metenda dhambi wakati huu.[c]
Yehova ni mwadilifu,[d] na mimi
na watu wangu tumekosea.
28 Msihi Yehova ili mingurumo
hii ya Mungu na mvua yake ya
mawe[e] ziishie hapo. Ndipo nita-
kuwa tayari kuwaruhusu mwe-
nde zenu, nanyi hamtaendelea
kukaa zaidi." **29** Basi Musa
akamwambia: "Mara tu nita-
kapoondoka jijini nitamnyoo-
shea Yehova mikono yangu.[f] Mi-
ngurumo itakoma nayo mvua
ya mawe haitaendelea tena, ili
upate kujua kwamba dunia ni
ya Yehova.[g] **30** Na wewe, pa-
moja na watumishi wako, taya-
ri ninajua kwamba hata waka-
ti huo hamtaonyesha woga wo-
wote kwa sababu ya Yehova
Mungu."[h]
31 Kama ilivyokuwa, kitani
na shayiri zilikuwa zimepi-
gwa, kwa sababu shayiri ili-
kuwa na masuke nacho kita-
ni kilikuwa na matumba ya
maua.[i] **32** Lakini ngano na
kusemethi[j] hazikuwa zimepi-
gwa, kwa sababu majira yake
yalikuwa hayajafika. **33** Sasa
Musa akaondoka jijini kutoka
kwa Farao, akamnyooshea Ye-
hova mikono yake, nayo mingu-
rumo na mvua ya mawe zika-
anza kukoma na mvua haiku-
nyesha juu ya dunia.[k] **34** Fa-
rao alipoona kwamba mvua na
mawe ya mvua na mingurumo
zilikuwa zimekoma, akatenda
dhambi tena na kuufanya
moyo wake uwe mgumu,[l] yeye

na watumishi wake. **35** Nao moyo wa Farao ukaendelea kuwa mkaidi, naye hakuwaruhusu wana wa Israeli waende zao, kama vile Yehova alivyokuwa amesema kupitia Musa.[a]

10 Ndipo Yehova akamwambia Musa: "Ingia ndani kwa Farao, kwa sababu mimi —mimi nimeuacha moyo wake na mioyo ya watumishi wake iwe migumu,[b] ili niweke ishara zangu hizi mbele yake,[c] **2** na ili upate kutangaza masikioni mwa mwana wako na mwana wa mwana wako jinsi ambavyo nimeshughulika vikali na Misri na ishara zangu ambazo nimesimamisha katikati yao;[d] nanyi hakika mtajua kwamba mimi ni Yehova."[e]

3 Basi Musa na Haruni wakaingia ndani kwa Farao na kumwambia: "Hivi ndivyo Yehova Mungu wa Waebrania amesema, 'Utaendelea kukataa kujitiisha kwangu mpaka wakati gani?[f] Waruhusu watu wangu waende zao ili wanitumikie. **4** Kwa maana ikiwa utaendelea kukataa kuwaruhusu watu wangu waende zao, tazama, kesho nitaleta nzige ndani ya mipaka yako.[g] **5** Nao watafunika uso wa dunia unaoonekana wala haitawezekana kuiona dunia; nao watakula kilichobaki, kile ambacho mvua ya mawe iliwaachia ninyi, nao watakula miti yenu yote inayochipuka shambani.[h] **6** Nazo nyumba zako na nyumba za watumishi wako wote na nyumba za Misri yote zitajaa kwa kadiri ambayo baba zako na baba za baba zako hawajapata kuona tangu siku za kuwako kwao juu ya nchi mpaka leo hii.'"[i] Kisha akageuka na kuondoka kwa Farao.[j]

SURA 9
a Kut 7:4
Kut 8:15

SURA 10
b Kut 4:21
Kut 9:34
Zb 7:11
c Kut 7:4
Kut 9:16
1Sa 4:8
Zb 78:12
Zb 135:9
Ro 9:17
d Kut 13:8
Kum 4:9
Kum 6:21
Zb 44:1
Zb 78:5
Yoe 1:3
e Kut 6:3
f Kut 9:17
Kut 16:28
Met 18:12
Isa 2:11
Yer 13:18
g Zb 78:46
Zb 105:34
Met 30:27
Yoe 1:4
h Kut 9:32
Zb 105:35
Yoe 2:3
i Kut 9:24
Yoe 2:9
j Kut 11:8
Ebr 11:27

Safu ya 2
a Met 29:6
b Zb 107:34
c Kut 12:31
d Kum 31:12
Zb 148:12
e Mwa 46:6
Mwa 50:8
Kut 10:26
f Kut 3:18
Kut 5:1
g Kut 12:31
h 2Nya 32:15
i Kut 10:28
j Kut 7:19
k Kum 28:38
Yoe 2:3
l Mwa 41:6
Kut 14:21
Zb 78:26
Yon 4:8
m Zb 78:46
Zb 105:34

7 Baada ya hapo watumishi wa Farao wakamwambia: "Mtu huyu ataendelea kuwa mtego[a] kwetu mpaka wakati gani? Waruhusu watu waende zao ili wamtumikie Yehova Mungu wao. Je, bado hujajua kwamba Misri imeangamia?"[b] **8** Kwa hiyo Musa na Haruni wakarudishwa kwa Farao, naye akawaambia: "Nendeni, mkamtumikie Yehova Mungu wenu.[c] Ni nani hasa wanaoenda?" **9** Ndipo Musa akasema: "Tutaenda pamoja na vijana wetu na wazee wetu. Tutaenda pamoja na wana wetu na binti[d] zetu, pamoja na kondoo zetu na ng'ombe zetu,[e] kwa maana tuna sherehe ya kumfanyia Yehova."[f] **10** Naye akawajibu: "Na iwe hivyo, kwamba Yehova yuko pamoja nanyi wakati nitakapowaruhusu ninyi na watoto wenu mwende zenu![g] Tazama, tofauti na hilo, mna lengo la kufanya jambo baya.[h] **11** Hapana! Nendeni, tafadhali, ninyi wanaume, mkamtumikie Yehova, kwa sababu hilo ndilo mnalotaka kupata." Ndipo wakafukuzwa kutoka mbele ya Farao.[i]

12 Sasa Yehova akamwambia Musa: "Unyooshe[j] mkono wako juu ya nchi ya Misri kwa ajili ya nzige, ili waje juu ya nchi ya Misri na kula mimea yote ya nchi, kila kitu ambacho ile mvua ya mawe iliacha."[k] **13** Mara moja Musa akainyoosha fimbo yake juu ya nchi ya Misri, naye Yehova akafanya upepo wa mashariki[l] uvume juu ya nchi siku hiyo yote na usiku wote. Asubuhi ikafika nao upepo wa mashariki ukawaleta hao nzige. **14** Nao nzige wakaanza kuja juu ya nchi yote ya Misri na kutua juu ya eneo lote la Misri.[m] Walikuwa

wenye kulemea sana.[a] Kabla yao hawakuwa wametokea kamwe jinsi hiyo nzige wengine kama wao, wala hakutatokea wowote kamwe jinsi hiyo baada yao. **15** Nao wakaufunika uso unaoonekana wa nchi[b] yote, nayo nchi ikawa na giza;[c] nao wakawa wakila mimea yote ya nchi na matunda yote ya miti ambayo ile mvua ya mawe ilikuwa imeacha;[d] wala hakikubaki chochote cha kijani kibichi juu ya miti wala juu ya mimea ya shambani katika nchi yote ya Misri.[e]

16 Basi Farao akawaita haraka haraka Musa na Haruni na kusema: "Nimemtendea dhambi Yehova Mungu wenu na ninyi pia.[f] **17** Na sasa mnisamehe,[g] tafadhali, dhambi yangu mara hii moja tu na kumsihi[h] Yehova Mungu wenu apate kuniondolea pigo hili lenye kufisha." **18** Basi akaondoka kwa Farao na kumsihi Yehova.[i] **19** Kisha Yehova akageuza upepo mkali sana wa magharibi, nao ukawaondolea mbali nzige hao na kuwapeleka katika Bahari Nyekundu. Hakuna nzige hata mmoja aliyeachwa abaki katika eneo lote la Misri. **20** Hata hivyo, Yehova akauacha moyo wa Farao uwe mkaidi,[j] naye hakuwaruhusu wana wa Israeli waende zao.

21 Kisha Yehova akamwambia Musa: "Unyooshe mkono wako kuelekea mbinguni,[k] ili giza lipate kutokea juu ya nchi ya Misri nalo giza liweze kuguswa." **22** Mara moja Musa akanyoosha mkono wake kuelekea mbinguni, na giza zito likaanza kutokea katika nchi yote ya Misri kwa siku tatu.[l] **23** Hawakuonana, wala hakuna yeyote kati yao aliyeondoka mahali pake kwa siku tatu; lakini kwa wana wote wa Israeli kulikuwa na nuru katika makao yao.[a] **24** Kisha Farao akamwita Musa na kusema: "Nendeni, mkamtumikie Yehova.[b] Ni kondoo zenu na ng'ombe zenu tu watakaozuiwa. Watoto wenu pia wanaweza kwenda pamoja nanyi."[c] **25** Lakini Musa akasema: "Wewe mwenyewe pia utatupa mikononi mwetu dhabihu na matoleo ya kuteketezwa, kwa maana tutavitoa kwa Yehova Mungu wetu.[d] **26** Na mifugo yetu pia itaenda pamoja nasi.[e] Hakuna hata ukwato utakaoruhusiwa kubaki, kwa sababu ni kutoka kati yao kwamba tutachukua baadhi yao ili kumwabudu Yehova Mungu wetu,[f] nasi wenyewe hatujui tutakachotoa katika ibada kwa Yehova mpaka tufike huko."[g] **27** Ndipo Yehova akauacha moyo wa Farao uwe mkaidi, wala hakukubali kuwaruhusu waende zao.[h] **28** Basi Farao akamwambia: "Toka mbele yangu![i] Jiangalie! Usijaribu kuuona uso wangu tena, kwa sababu siku utakayouona uso wangu utakufa."[j] **29** Ndipo Musa akasema: "Kama ambavyo umesema na iwe. Sitajaribu kuuona uso wako tena."[k]

11 Na Yehova akamwambia Musa: "Nitaleta pigo moja zaidi juu ya Farao na Misri. Halafu atawaruhusu mwende zenu kutoka hapa.[l] Wakati atakapowaruhusu mwende zenu nyote kabisa, atawafukuza kutoka hapa.[m] **2** Sasa, sema masikioni mwa watu, kwamba kila mwanamume na amwombe mwenzake na kila mwanamke na amwombe mwenzake

SURA 10
a Kut 10:5
b Yoe 1:6
c Yoe 2:10
d Zb 105:35
e Yoe 1:7
Yoe 2:3
f Kut 9:27
1Sa 26:21
g Zb 76:12
h Kut 9:28
1Fa 13:6
Mdo 8:24
i Kut 8:30
j Kut 7:3
Kut 11:10
Yoh 12:40
Ro 9:18
k Kut 8:5
l Zb 105:28
Amo 5:8

Safu ya 2
a Kut 8:22
Kut 9:6
Kut 9:26
Mal 3:18
b Kut 8:28
Kut 9:28
c Mwa 34:23
Kut 10:10
d Kut 3:18
Kut 5:3
Kut 8:27
e Kut 12:32
f Mal 1:11
g Met 3:9
h Kut 4:21
Kut 14:4
Ro 9:18
i Kut 10:11
j 2Nya 16:10
k Ebr 11:27

SURA 11
l Kut 12:31
Kum 4:34
m Kut 3:20
Kut 12:32

vyombo vya fedha na vyombo vya dhahabu."[a] **3** Basi Yehova akawapa watu kibali machoni pa Wamisri.[b] Mwanamume huyo Musa pia alikuwa mkuu sana katika nchi ya Misri, machoni pa watumishi wa Farao na machoni pa watu.[c]

4 Na Musa akasema: "Hivi ndivyo Yehova amesema, 'Karibu na katikati ya usiku hivi nitaingia katikati ya Misri,[d] **5** na kila mzaliwa wa kwanza[e] katika nchi ya Misri atakufa, tokea mzaliwa wa kwanza wa Farao anayeketi juu ya kiti chake cha ufalme hata mzaliwa wa kwanza wa mjakazi aliye kwenye jiwe la kusagia la mkononi na kila mzaliwa wa kwanza wa mnyama.[f] **6** Na hakika kutatokea kilio kikubwa katika nchi yote ya Misri, ambacho namna yake haijatokea kamwe, na ambacho namna yake haitatokea kamwe.[g] **7** Lakini hakuna mbwa yeyote atakayeuchezesha ulimi wake kwa bidii dhidi ya yeyote wa wana wa Israeli, kuanzia mwanadamu hata mnyama;[h] ili mpate kujua kwamba Yehova anaweza kufanyiza tofauti kati ya Wamisri na wana wa Israeli.'[i] **8** Na hakika hawa watumishi wako wote watanijia na kusujudu mbele yangu,[j] na kusema, 'Nenda, wewe na watu wote wanaofuata hatua zako.' Na baada ya hapo mimi nitaondoka." Kisha akaondoka mbele ya Farao akiwaka hasira.

9 Ndipo Yehova akamwambia Musa: "Farao hatawasikiliza ninyi,[k] ili miujiza yangu iongezeke katika nchi ya Misri."[l] **10** Na Musa na Haruni wakafanya miujiza yote hiyo mbele ya Farao;[m] lakini Yehova alikuwa akiuacha moyo wa Farao uwe mkaidi, hivi kwamba hakuwaruhusu wana wa Israeli waende zao kutoka katika nchi yake.[a]

12 Yehova akasema na Musa na Haruni katika nchi ya Misri: **2** "Mwezi huu utakuwa mwanzo wa miezi kwenu. Utakuwa mwezi wa kwanza wa mwaka kwenu.[b] **3** Sema na kusanyiko lote la Israeli, na kuwaambia, 'Siku ya kumi ya mwezi huu watajichukulia kila mmoja kondoo[c] kwa ajili ya nyumba ya mababu, kondoo mmoja kwa kila nyumba. **4** Lakini ikiwa nyumba hiyo ni ndogo sana kwa kondoo huyo, basi yeye na jirani yake aliye karibu watamwingiza nyumbani mwake kulingana na hesabu ya nafsi; mtafanya hesabu ya kila mmoja kulingana na ulaji wake kuhusiana na kondoo huyo. **5** Kondoo huyo anapaswa kuwa asiye na kasoro,[d] dume, mwenye umri wa mwaka mmoja, kwa ajili yenu.[e] Mnaweza kumchagua kutoka kati ya wana-kondoo dume au kutoka kati ya mbuzi. **6** Naye ataendelea kukaa chini ya ulinzi wenu mpaka siku ya kumi na nne ya mwezi huu,[f] nalo kutaniko zima la kusanyiko la Israeli litamchinja katikati ya zile jioni mbili.[g] **7** Nao watachukua sehemu ya damu na kuipaka juu ya miimo miwili ya mlango na sehemu ya juu ya mlango wa nyumba ambamo watamla.[h]

8 "'Nao wataila hiyo nyama usiku huu.[i] Wataila ikiwa imechomwa kwa moto pamoja na keki zisizo na chachu[j] na pia mboga chungu za majani.[k] **9** Msile yoyote ya hiyo ikiwa mbichi au ikiwa imetokoswa, ikiwa imepikwa ndani ya

SURA 11
a Kut 3:22; Kut 12:35; Zb 105:37; Met 13:22
b Kut 3:21; Kut 12:36
c 2Sa 7:9; Est 9:4; Mdo 7:22
d Kut 12:29; Amo 4:10
e Kut 4:23; Kut 13:15; Zb 78:51; Zb 105:36; Zb 136:10; Ebr 11:28
f Kut 12:12; Zb 135:8
g Kut 12:30
h Yos 10:21
i Kut 8:22; Kut 9:4; Kut 10:23; Kut 12:13; Zb 91:7; Mal 3:18
j Kut 12:33
k Kut 3:19; Kut 7:4; Ro 9:18
l Kut 7:3; Yer 32:20
m Zb 135:9

Safu ya 2
a Kut 4:21; Kut 9:16; Kut 10:20; 1Sa 6:6; Isa 26:10

SURA 12
b Kut 13:4; Kut 23:15; Kut 34:18; Hes 28:16; Kum 16:1; Est 3:7
c Mwa 22:8; Yoh 1:29; 1Ko 5:7; Ufu 5:6; Ufu 7:10
d Law 22:19; Kum 17:1; Mal 1:14; Ebr 7:26; Ebr 9:14; 1Pe 1:19
e Law 1:3; Law 23:12
f Hes 28:16; Eze 45:21
g Kut 12:18; Kut 16:12; Law 23:5; Hes 9:3; Kum 16:6
h 1Ko 5:7; Efe 1:7; Ebr 11:28; 1Pe 1:2
i Kum 16:7; Mt 26:17
j Kut 13:3; Kut 34:25; Kum 16:3; 1Ko 5:8
k Kut 1:14; Hes 9:11

maji, bali ikiwa imechomwa
kwa moto, kichwa chake pamo-
ja na miguu yake na matumbo
yake. **10** Nanyi hamtaacha
yoyote mpaka asubuhi, lakini
yoyote itakayobaki mpaka asu-
buhi mtaiteketeza kwa moto.[a]
11 Na hivi ndivyo mtakavyo-
kula, viuno vyenu vikiwa vi-
mefungwa mshipi,[b] viatu[c] vi-
kiwa miguuni penu na fimbo
yenu mkononi mwenu; nanyi
mtaila haraka haraka. Ni pa-
saka ya Yehova.[d] **12** Nami ni-
tapita katikati ya nchi ya Mi-
sri usiku huu[e] na kumpiga kila
mzaliwa wa kwanza katika nchi
ya Misri, kuanzia mwanadamu
hata mnyama;[f] nami nitateke-
leza hukumu[g] juu ya miungu
yote ya Misri. Mimi ni Yeho-
va.[h] **13** Na damu hiyo itaku-
wa ishara yenu juu ya nyumba
mtakazokuwamo; nami nitaio-
na damu hiyo na kupita juu
yenu,[i] nalo pigo halitakuja juu
yenu kama uharibifu ninapoipi-
ga nchi ya Misri.

14 "'Na siku hii itakuwa uku-
mbusho kwenu, nanyi mtaishe-
rehekea ikiwa sherehe kwa Ye-
hova katika vizazi vyenu vyo-
te. Nanyi mtaisherehekea kama
sheria mpaka wakati usio na
kipimo. **15** Siku saba mtaku-
la keki zisizo na chachu. Ndi-
yo, siku ya kwanza mtaondoa
unga uliokandwa wenye chachu
kutoka katika nyumba zenu,
kwa sababu mtu yeyote anaye-
kula kitu kilicho na chachu, ku-
anzia siku ya kwanza mpaka
siku ya saba,[j] nafsi hiyo itakati-
liwa mbali kutoka katika Israe-
li.[k] **16** Na siku ya kwanza ku-
takuwa na mkusanyiko mtaka-
tifu kwa ajili yenu, na siku ya
saba mkusanyiko mtakatifu.[l]
Hakuna kazi yoyote itakayofa-
nywa katika siku hizo.[m] Ila tu
kile ambacho kila nafsi inahita-
ji kula, hicho tu kinaweza kufa-
nywa kwa ajili yenu.[a]

17 "'Nanyi lazima mshike
sherehe ya keki zisizo na cha-
chu,[b] kwa sababu siku hiyo hiyo
nitayatoa majeshi yenu kuto-
ka katika nchi ya Misri. Na-
nyi mtaishika siku hiyo katika
vizazi vyenu vyote, kama she-
ria mpaka wakati usio na ki-
pimo. **18** Katika mwezi wa
kwanza, siku ya 14 ya mwezi
huo, wakati wa jioni mtakula
keki zisizo na chachu mpaka
siku ya 21 ya mwezi wakati wa
jioni.[c] **19** Siku saba unga wo-
wote uliokandwa wenye cha-
chu usipatikane katika nyu-
mba zenu, kwa sababu mtu ye-
yote anayeonja kitu kilicho
na chachu, awe mkaaji mgeni
au mwenyeji wa nchi,[d] nafsi
hiyo itakatiliwa mbali kuto-
ka katika kusanyiko la Israeli.[e]
20 Hamtakula kitu chochote
kilicho na chachu. Katika ma-
kao yenu yote mtakula keki zi-
sizo na chachu.'"

21 Papo hapo Musa akawaita
wanaume wote wazee wa
Israeli[f] na kuwaambia: "Toe-
ni na kujichukulia kondoo na
mbuzi kulingana na familia
zenu, na kuchinja mnyama wa
pasaka.[g] **22** Nanyi mtachu-
kua tawi la hisopo[h] na kulicho-
vya katika damu iliyo ndani ya
beseni na kuipaka sehemu ya
juu ya mlango na juu ya ile mi-
imo miwili ya mlango kwa kia-
si fulani cha damu iliyo kwenye
beseni; na yeyote kati yenu asi-
toke nje ya mlango wa nyumba
yake mpaka asubuhi. **23** Ki-
sha Yehova atakapopita katika-
ti ili kuwaletea pigo Wamisri
na kuiona damu kwenye sehe-
mu ya juu ya mlango na kwenye

SURA 12
a Law 7:15
Law 22:30
Kum 16:4
b Lu 12:35
Efe 6:14
1Pe 1:13
c Efe 6:15
d Hes 28:16
Kum 16:6
e Kut 11:4
Amo 5:17
f Kut 11:5
Kut 12:29
g Hes 33:4
Isa 19:1
Yer 43:13
Sef 2:11
h 1Ko 8:6
i Mt 20:28
Ro 5:9
Ebr 11:28
1Yo 1:7
j Kut 23:15
Law 23:6
k Hes 9:13
l Law 23:4
m Law 23:8

Safu ya 2
a Mt 12:1
b Law 23:6
Lu 22:1
1Ko 5:8
c Law 23:5
Law 23:6
Eze 45:21
d Kut 12:49
Hes 9:14
Kum 16:3
1Ko 5:7
e Hes 9:13
f Kut 3:16
Kut 19:7
Hes 11:16
g Hes 9:2
Yos 5:10
2Fa 23:21
2Nya 35:6
Ezr 6:20
Lu 22:7
h Law 14:6
Zb 51:7
Ebr 9:19

ile miimo miwili ya mlango, hakika Yehova atapita juu ya mlango, naye hataruhusu uharibifu uingie ndani ya nyumba zenu na kuwaletea pigo.[a]
24 "Nanyi mtashika jambo hili kama sharti[b] kwa ajili yenu na wana wenu mpaka wakati usio na kipimo.[c] **25** Na itakuwa kwamba mtakapoingia katika nchi ambayo Yehova atawapa, kama alivyosema, basi mtaendelea kuufanya utumishi huu.[d] **26** Na itakuwa kwamba wana wenu watakapowaambia, 'Utumishi huu unamaanisha nini kwenu?'[e] **27** ndipo mtakaposema, 'Ni dhabihu ya pasaka kwa Yehova,[f] aliyepita juu ya nyumba za wana wa Israeli huko Misri alipowaletea Wamisri pigo, lakini akazikomboa nyumba zetu.'"

Kisha watu hao wakainama na kusujudu.[g] **28** Kisha wana wa Israeli wakaenda na kufanya kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa na Haruni.[h] Wakafanya vivyo hivyo.
29 Na ikawa kwamba katikati ya usiku Yehova akampiga kila mzaliwa wa kwanza katika nchi ya Misri,[i] kuanzia mzaliwa wa kwanza wa Farao anayeketi juu ya kiti cha ufalme kufikia mzaliwa wa kwanza wa mateka aliye gerezani, na kila mzaliwa wa kwanza wa mnyama.[j] **30** Kisha Farao akaamka usiku, yeye na watumishi wake wote na Wamisri wengine wote; na kukaanza kutokea kilio kikubwa kati ya Wamisri,[k] kwa sababu hapakuwa na nyumba yoyote ambamo hamkuwa na mtu aliyekufa. **31** Ndipo akamwita[l] Musa na Haruni mara moja wakati wa usiku na kusema: "Simameni, tokeni kati ya watu wangu, ninyi na wale wana wengine wa Israeli, na mwende, mkamtumikie Yehova, kama mlivyosema.[a]
32 Chukueni makundi yenu na mifugo yenu, kama mlivyosema,[b] na mwende. Pia, mnibariki mimi vilevile."
33 Na Wamisri wakaanza kuwahimiza watu ili wawafukuze haraka[c] kutoka katika nchi hiyo, "kwa sababu," walisema, "sisi sote ni kana kwamba tumekufa!"[d] **34** Basi watu wakachukua unga wao wa kukandwa kabla haujachacha, pamoja na vikandio vyao vikiwa vimefungwa katika nguo zao za kujitanda begani mwao.
35 Na wana wa Israeli wakafanya kulingana na neno la Musa, wakawaomba Wamisri vyombo vya fedha na vyombo vya dhahabu na nguo za kujitanda.[e]
36 Naye Yehova akawapa watu hao kibali machoni pa Wamisri,[f] hivi kwamba hao wakawapa walichoomba;[g] nao wakawaacha Wamisri bila chochote.[h]
37 Na wana wa Israeli wakaondoka Ramesesi[i] kuelekea Sukothi,[j] kufikia hesabu ya wanaume mia sita elfu wanaotembea kwa miguu, bila kuhesabu watoto.[k] **38** Na jamii kubwa iliyochangamana[l] pia ikaenda pamoja nao, na makundi na mifugo vilevile, kundi la wanyama wengi sana. **39** Nao wakaanza kuoka unga uliokandwa waliokuwa wameuchukua kutoka Misri uwe keki za mviringo, keki zisizo na chachu, kwa sababu haukuwa umechacha, kwa sababu walikuwa wamefukuzwa kutoka Misri nao hawakuweza kukawia na pia hawakuwa wamejitayarishia vyakula vyovyote.[m]
40 Na kukaa kwa wana wa Israeli, waliokuwa wamekaa[n]

SURA 12
a Isa 37:36; Eze 9:6; Ebr 11:28
b Law 23:4; Kum 16:3
c Efe 2:15; Kol 2:14; Ebr 8:13
d Yos 5:10; Zb 105:45
e Kut 13:8; Kum 6:7; Yos 4:6; Zb 78:6; Zb 145:4; Efe 6:4
f Kut 34:25; Kum 16:2; 1Ko 5:7
g Kut 4:31; Ne 8:6
h Ebr 11:28
i Mwa 15:14; Hes 33:4; Zb 78:51; Zb 105:36; Zb 136:10; Ebr 11:28
j Kut 11:5; Hes 3:13; Zb 135:8
k Kut 11:6
l Kut 10:29

Safu ya 2
a Kut 3:20; Kut 6:1; Kut 10:9; Zb 105:38
b Kut 10:26
c Kut 12:11
d Mwa 20:3; Kut 10:7; Hes 17:12
e Mwa 15:14; Kut 3:21; Kut 11:2; Zb 105:37
f Kut 11:3; Met 16:7
g Kum 15:15
h Kut 3:22
i Mwa 47:11; Kut 1:11
j Hes 33:5
k Mwa 12:2; Mwa 15:5; Mwa 46:3; Kut 1:7; Kut 38:26; Hes 2:32; Hes 11:21
l Hes 11:4; Zek 8:23
m Kut 6:1; Kut 11:1; Kut 12:31
n Mwa 12:4; Mwa 21:5; Mwa 25:26; Mwa 47:9

katika Misri,[a] kulikuwa miaka 430.[b] **41** Na ikawa kwamba mwishoni mwa ile miaka 430, naam, ikawa kwamba siku hiyo hiyo majeshi yote ya Yehova yakatoka katika nchi ya Misri.[c] **42** Ni usiku wa kuadhimishwa kuhusiana na Yehova kwa kuwatoa katika nchi ya Misri. Kuhusiana na Yehova usiku huu ni usiku wa kuadhimishwa kwa wana wote wa Israeli katika vizazi vyao.[d]

43 Na Yehova akamwambia Musa na Haruni: "Hii ndiyo sheria ya pasaka:[e] Hakuna mgeni yeyote atakayeila.[f] **44** Lakini palipo na mtumwa yeyote aliyenunuliwa kwa pesa, utamtahiri.[g] Ndipo atashiriki kuila. **45** Mhamiaji na mfanyakazi wa kukodiwa hatakula. **46** Italiwa katika nyumba moja. Hutatoa nyama yoyote nje ya nyumba hiyo na kuipeleka mahali fulani nje. Wala hamtavunja mfupa wake wowote ndani yake.[h] **47** Kusanyiko lote la Israeli litaisherehekea.[i] **48** Na ikiwa mkaaji mgeni anakaa pamoja nawe akiwa mgeni naye atasherehekea pasaka kwa Yehova, kila mwanamume wa kwake na atahiriwe.[j] Ndipo apate kukaribia ili kuisherehekea; na awe kama mwenyeji wa nchi. Bali mwanamume yeyote ambaye hajatahiriwa asipate kuila. **49** Sheria moja itakuwapo kwa ajili ya mwenyeji na kwa ajili ya mkaaji mgeni anayekaa akiwa mgeni katikati yenu."[k]

50 Basi wana wote wa Israeli wakafanya kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa na Haruni. Walifanya vivyo hivyo.[l] **51** Na ikawa siku hiyo hiyo kwamba Yehova akawatoa wana wa Israeli pamoja na majeshi[a] yao kutoka katika nchi ya Misri.

13 Na Yehova akanena zaidi na Musa, na kusema: **2** "Nitakasie kila mzaliwa wa kwanza wa kiume anayefungua kila tumbo la uzazi kati ya wana wa Israeli, kati ya wanadamu na wanyama. Ni wangu."[b]

3 Naye Musa akawaambia watu: "Na ikumbukwe siku hii ambayo mlitoka Misri,[c] katika nyumba ya watumwa, kwa sababu kwa nguvu za mkono Yehova aliwatoa hapa.[d] Basi chochote kilicho na chachu kisiliwe.[e] **4** Leo mnaondoka katika mwezi wa Abibu.[f] **5** Na itakuwa kwamba Yehova atakapokuwa amekuingiza katika nchi ya Wakanaani na Wahiti na Waamori na Wahivi na Wayebusi,[g] ambayo aliwaapia mababu zako kuwa atakupa,[h] nchi inayotiririka maziwa na asali,[i] ndipo utatoa utumishi huu katika mwezi huu. **6** Siku saba utakula keki zisizo na chachu,[j] na katika siku ya saba ni sherehe kwa Yehova.[k] **7** Keki zisizo na chachu zitaliwa kwa siku hizo saba;[l] na chochote kilicho na chachu kisionekane kwako,[m] wala unga wowote uliokandwa wenye chachu usionekane kwako ndani ya mipaka yako yote.[n] **8** Nawe utamwambia mwana wako siku hiyo, na kusema, 'Ni kwa sababu ya jambo ambalo Yehova amenifanyia nilipotoka Misri.'[o] **9** Nayo itatumika kwako kama ishara mkononi mwako na ukumbusho katikati ya macho yako,[p] ili sheria ya Yehova iwe katika kinywa chako;[q] kwa sababu kwa mkono wenye nguvu Yehova alikutoa Misri.[r]

SURA 12

a Mwa 46:3
Mwa 47:27
Mdo 13:17
b Mwa 15:13
Mdo 7:6
Ga 3:17
c Kut 7:4
d Kut 12:14
Kum 16:1
e Law 23:5
Hes 9:14
Kum 16:2
Yos 5:10
Mk 14:1
1Ko 5:7
f Law 22:10
Efe 2:12
g Mwa 17:12
Mwa 17:23
h Hes 9:12
Zb 34:20
Yoh 19:33
Yoh 19:36
i Hes 9:14
j Mwa 17:12
k Law 24:22
Hes 15:16
Ga 3:28
Kol 3:11
l Kut 7:6
Kut 39:32
Kum 12:32

Safu ya 2

a Kut 6:26
Kut 13:18

SURA 13

b Law 27:26
Hes 3:13
Hes 18:15
Kum 15:19
Lu 2:23
c Kut 12:42
Kum 16:3
d Kut 6:1
Kum 4:34
Ne 9:10
e Kut 12:20
1Ko 5:7
f Kut 23:15
Kut 34:18
Kum 16:1
g Kut 3:8
Kut 34:11
1Fa 9:20
h Mwa 15:18
Kut 6:8
Mdo 7:5
i Kut 3:17
Kum 6:3
Kum 8:8
j Kut 12:15
Kut 34:18
1Ko 5:8
k Kut 10:9
Law 23:8
Lu 22:1
l Kut 23:15
m Kum 16:3
n Kut 12:19
o Kut 12:27
p Kut 12:14
Kum 6:8
Kum 11:18
q Met 23:16
r Kut 6:1
Kut 7:4

10 Nawe lazima uishike sheria hii kwa wakati wake uliowekwa mwaka baada ya mwaka.[a]

11 "Na itakuwa kwamba wakati Yehova anapokuingiza katika nchi ya Wakanaani,[b] kama alivyokuapia wewe na mababu zako,[c] na wakati anapokupa hiyo, **12** ndipo lazima umtoe kila anayefungua tumbo la uzazi kwa ajili ya Yehova,[d] na kila mzaliwa wa kwanza, mtoto wa mnyama,[e] ambaye atakuwa mali yako. Walio wa kiume ni wa Yehova.[f] **13** Na kila mzaliwa wa kwanza wa punda utamkomboa kwa kondoo, nawe usipomkomboa, basi utaivunja shingo yake.[g] Na kila mzaliwa wa kwanza wa mwanadamu kati ya wana wako utamkomboa.[h]

14 "Na itakuwa kwamba ikiwa mwana wako atakuuliza baadaye,[i] na kusema, 'Hili linamaanisha nini?' basi utamwambia, 'Kwa nguvu za mkono, Yehova alitutoa Misri,[j] katika nyumba ya watumwa.[k] **15** Na ikawa kwamba Farao alipoonyesha ukaidi kwa kukataa kuturuhusu twende zetu,[l] ndipo Yehova akamuua kila mzaliwa wa kwanza katika nchi ya Misri,[m] kuanzia mzaliwa wa kwanza wa mwanadamu kufikia mzaliwa wa kwanza wa mnyama.[n] Ndiyo sababu mimi ninamtolea Yehova dhabihu wote wa kiume wanaofungua tumbo la uzazi,[o] na kila mzaliwa wa kwanza wa wanangu ninamkomboa.'[p] **16** Nayo itatumika kuwa ishara mkononi mwako na utepe wa kipaji katikati ya macho yako,[q] kwa sababu kwa nguvu za mkono Yehova alitutoa Misri."[r]

17 Na ikawa kwamba wakati Farao alipowaruhusu watu waende zao, Mungu hakuwaongoza kupitia njia ya nchi ya Wafilisti kwa kuwa tu ilikuwa karibu, kwa maana Mungu alisema: "Huenda hao watu watajuta watakapoona vita nao hakika watarudi Misri."[a] **18** Basi Mungu akawafanya watu wazunguke kupitia njia ya nyika ya Bahari Nyekundu.[b] Hata hivyo wana wa Israeli walitoka nchini Misri wakiwa wamejipanga kivita.[c] **19** Na Musa akaichukua mifupa ya Yosefu pamoja naye, kwa sababu alikuwa amewafanya wana wa Israeli waape rasmi, na kusema: "Bila shaka Mungu atawaelekezea ninyi fikira,[d] nanyi lazima mwichukue mifupa yangu kutoka hapa pamoja nanyi."[e] **20** Nao wakaondoka Sukothi na kupiga kambi katika Ethamu ukingoni mwa nyika.[f]

21 Naye Yehova alikuwa akienda mbele yao wakati wa mchana katika nguzo ya wingu ili kuwaongoza njiani,[g] na wakati wa usiku katika nguzo ya moto ili kuwapa nuru ya kwenda wakati wa mchana na wakati wa usiku.[h] **22** Ile nguzo ya wingu haikuondoka mbele ya watu wakati wa mchana wala ile nguzo ya moto wakati wa usiku.[i]

14 Sasa Yehova akasema na Musa, na kumwambia: **2** "Sema na wana wa Israeli, kwamba warudi na kupiga kambi mbele ya Pihahirothi katikati ya Migdoli na bahari, kukabili Baal-sefoni.[j] Mbele yake mtapiga kambi kando ya bahari. **3** Kisha Farao hakika atasema kuhusu wana wa Israeli, 'Wanatanga-tanga nchini kwa kuvurugika. Nyika imewazingira.'[k] **4** Kwa hiyo, kwa

SURA 13
a Kut 12:24 Kut 23:15 Law 23:6 Kum 16:3
b Ne 9:24
c Mwa 15:18 Zb 105:42
d Hes 3:13
e Law 27:26
f Kut 22:29 Kut 34:19 Hes 8:17 Kum 15:19 Lu 2:23
g Kut 34:20
h Hes 18:15
i Kut 12:26 Kum 6:20 Zb 145:4
j Kum 26:8
k Kum 7:8
l Kut 5:2
m Zb 78:51 Zb 135:8
n Kut 11:5 Kut 12:29
o Kut 13:2 Kut 13:12 Kum 21:17
p Kut 6:6
q Kum 6:8 Kum 11:18
r Kut 6:1 Yud 5

Safu ya 2
a Kut 14:11 Kut 16:3 Hes 14:3 Ne 9:17 Mdo 7:39
b Kut 14:2 Hes 33:5
c Kut 12:51
d Zb 135:4 Lu 1:68 Lu 7:16
e Mwa 50:25 Yos 24:32 Ebr 11:22
f Hes 33:6
g Kut 14:19 Hes 9:15 Kum 1:33 Ne 9:12 Zb 99:7
h Kut 14:24 Hes 14:14 Zb 78:14
i Zb 105:39 1Ko 10:1

SURA 14
j Kut 13:18 Hes 33:7
k Zb 71:11

kweli nitauacha moyo wa Farao
uwe mkaidi,[a] naye hakika ata-
wafuatilia wao nami nitajipa-
tia utukufu kupitia kwa Farao
na majeshi yake yote;[b] nao Wa-
misri watajua hakika kwamba
mimi ni Yehova."[c] Basi wakafa-
nya vivyo hivyo.
5 Baadaye mfalme wa Misri
akaambiwa kwamba watu wali-
kuwa wamekimbia na kwenda
zao. Mara moja moyo wa Fa-
rao na watu wake vilevile uka-
badilika kuhusiana na watu,[d]
kwa hiyo wakasema: "Tume-
fanya nini, kwa kuwaruhusu
Waisraeli waende zao, waa-
che kuwa watumwa[e] wetu?"
6 Kwa hiyo akatayarisha ma-
gari yake ya vita, na kuwachu-
kua watu wake pamoja naye.[f]
7 Naye akachukua magari mia
sita yaliyochaguliwa[g] na yale
magari mengine yote ya Misri
na mashujaa wa vita juu ya
kila moja la magari hayo.
8 Basi Yehova akauacha moyo
wa Farao mfalme wa Misri uwe
mkaidi,[h] naye akawafuatilia
wana wa Israeli, huku wana wa
Israeli wakienda kwa mkono
ulioinuliwa.[i] **9** Nao Wamisri
wakawafuatilia, na farasi wote
wa magari wa Farao na askari
wake wapanda-farasi[j] na maje-
shi yake wakawafikia walipoku-
wa wamepiga kambi kando ya
bahari, karibu na Pihahirothi,
kukabili Baal-sefoni.[k]
10 Farao alipokaribia, wana
wa Israeli wakaanza kuinua
macho yao, na tazama, Wami-
sri walikuwa wakipiga mwendo
wakiwafuatilia; na wana wa
Israeli wakaogopa sana na kua-
nza kumlilia Yehova.[l] **11** Nao
wakamwambia Musa: "Je, ni
kwa sababu hakuna makabu-
ri yoyote huko Misri ndiyo sa-
babu umetuleta hapa ili tufie
nyikani?[a] Ni nini hiki ambacho
umetutendea kwa kutuongoza
kutoka Misri? **12** Je, hili silo
neno tulilokuambia huko Mi-
sri, tukisema, 'Tuache, tuwa-
tumikie Wamisri'? Kwa maana
ni afadhali kwetu tuwatumikie
Wamisri kuliko kufa nyikani."[b]
13 Kisha Musa akawaambia
watu: "Msiogope.[c] Simameni
imara muuone wokovu wa Ye-
hova, atakaowafanyia ninyi
leo.[d] Kwa maana Wamisri mna-
owaona leo hamtawaona tena,
hasha, hamtawaona tena ka-
mwe.[e] **14** Yehova mwenyewe
atawapigania ninyi,[f] nanyi we-
nyewe mtakaa kimya."
15 Sasa Yehova akamwa-
mbia Musa: "Kwa nini unaende-
lea kunililia?[g] Waambie wana
wa Israeli kwamba wanapaswa
kuvunja kambi. **16** Wewe
nawe, inua fimbo[h] yako na kuu-
nyoosha mkono wako juu ya
bahari, uitenganishe,[i] ili wana
wa Israeli wapate kupita kati-
kati ya bahari juu ya nchi kavu.[j]
17 Mimi nami, tazama, nitaia-
cha mioyo ya Wamisri iwe mi-
kaidi,[k] ili waingie kuwafuati-
lia wao nami nijipatie utukufu
kupitia kwa Farao na majeshi
yake yote, magari yake ya vita
na askari wake wapanda-fara-
si.[l] **18** Na Wamisri hakika wa-
tajua kwamba mimi ni Yeho-
va nitakapojipatia utukufu ku-
pitia kwa Farao, magari yake
ya vita na askari wake wapa-
nda-farasi."[m]
19 Ndipo malaika[n] wa Mu-
ngu wa kweli aliyekuwa akie-
nda mbele ya kambi ya Isra-
eli akaondoka na kwenda nyu-
ma, nayo nguzo ya wingu ikao-
ndoka mbele yao na kusimama
nyuma yao.[o] **20** Kwa hiyo ika-
ingia katikati ya kambi ya

SURA 14
a Kut 4:21
Kut 7:13
Ro 9:18
b Kut 9:16
Kut 15:11
Kut 18:11
Yos 2:10
Ne 9:11
Isa 2:11
Ro 9:17
c Kut 7:5
Kut 8:22
Zb 83:18
Eze 26:6
d Kut 12:33
Zb 105:25
e Amu 6:8
1Sa 2:27
1Sa 6:6
f Kut 14:23
g Yos 17:16
Amu 4:3
h Kut 7:3
Kum 2:30
Yos 11:20
Zb 10:2
Met 16:18
i Hes 33:3
j Kut 15:19
k Kut 15:9
Yos 24:6
l Yos 24:7
Ne 9:9
Zb 34:17
Zb 107:6

Safu ya 2
a Kut 16:3
Kut 17:3
Hes 14:2
Zb 106:7
b Kut 5:21
Kut 6:9
Ebr 3:16
Ebr 10:38
c Hes 14:9
Kum 20:3
2Nya 20:15
Zb 27:1
Zb 46:1
Isa 41:10
d 2Nya 20:17
Met 29:25
e Kut 14:30
Kut 15:5
Zb 136:15
Met 16:4
Ne 9:11
f Kum 1:30
Kum 20:4
2Nya 20:29
g Yos 7:10
h Kut 4:20
Kut 17:9
i Zb 78:13
j Ne 9:11
k Kut 4:21
Kut 7:13
Ro 9:18
l Kut 9:16
Yos 24:6
Ro 9:17
m Kut 14:4
n Mwa 48:16
Kut 32:34
Hes 20:16
Yud 9
o Kut 13:21
Zb 34:7
Isa 52:12

Wamisri na kambi ya Israeli.[a] Kwa upande mmoja ikawa wingu pamoja na giza. Kwa upande ule mwingine ikawa ikiuangaza usiku.[b] Nacho kikundi hiki hakikukaribia kikundi kile usiku kucha.

21 Sasa Musa akanyoosha mkono wake juu ya bahari;[c] naye Yehova akaanza kuifanya bahari irudi nyuma kwa upepo wenye nguvu wa mashariki usiku kucha na kuligeuza bonde la bahari liwe nchi kavu,[d] nayo maji yalikuwa yakitenganishwa.[e] **22** Mwishowe wana wa Israeli wakapita katikati ya bahari juu ya nchi kavu,[f] huku maji yakiwa ukuta kwao mkono wao wa kuume na wa kushoto.[g] **23** Na Wamisri wakaanza kufuatilia, nao farasi wote wa Farao, magari yake ya vita na askari wake wapanda-farasi wakaanza kuingia baada yao,[h] kuingia katikati ya bahari. **24** Na ikawa kwamba wakati wa kesha la kuamkia asubuhi, Yehova akaanza kuiangalia kambi ya Wamisri kutoka ndani ya nguzo ya moto na wingu,[i] naye akaivuruga[j] kambi ya Wamisri. **25** Naye akawa akiyaondoa magurudumu kutoka kwenye magari yao hivi kwamba wakawa wakiyaendesha kwa shida;[k] nao Wamisri wakaanza kusema: "Na tukimbie tusikaribie Israeli hata kidogo, kwa sababu hakika Yehova anawapigania dhidi ya Wamisri."[l]

26 Mwishowe Yehova akamwambia Musa: "Unyooshe mkono wako juu ya bahari,[m] ili maji yarudi juu ya Wamisri, magari yao ya vita na askari wao wapanda-farasi." **27** Mara moja Musa akaunyoosha mkono wake juu ya bahari, nayo bahari ikaanza kurudia hali yake ya kawaida asubuhi ikikaribia. Wakati wote huo Wamisri walikuwa wakikimbia wasikutane nayo, lakini Yehova akawakung'uta Wamisri katikati ya bahari.[a] **28** Nayo maji yakaendelea kurudi.[b] Mwishowe yakafunika magari ya vita na askari wapanda-farasi wa majeshi yote ya Farao na ambao walikuwa wameingia baharini kuwafuatilia.[c] Hakuna hata mmoja kati yao aliyebaki.[d]

29 Nao wana wa Israeli, walitembea juu ya nchi kavu katikati ya sakafu ya bahari,[e] nayo maji yalikuwa kwao ukuta mkono wao wa kuume na wa kushoto.[f] **30** Basi siku hiyo Yehova akaokoa Israeli kutoka kwa mkono wa Wamisri,[g] na Israeli wakawaona Wamisri wakiwa wamekufa kando ya bahari.[h] **31** Israeli wakauona pia ule mkono mkuu ambao Yehova aliufanya utende juu ya Wamisri; nao watu wakaanza kumwogopa Yehova na kuwa na imani katika Yehova na katika Musa mtumishi wake.[i]

15 Wakati huo Musa na wana wa Israeli wakaanza kumwimbia Yehova wimbo huu na kusema yafuatayo:[j]

"Acheni nimwimbie
Yehova, kwa maana
ametukuzwa sana.[k]
Farasi na mpandaji wake
amewatupa baharini.[l]
2 Nguvu zangu na uwezo
wangu ni Yah,[m] kwa
maana yeye ndiye
wokovu wangu.[n]
Huyu ndiye Mungu wangu,
nami nitamsifu;[o] Mungu
wa baba yangu,[p] nami
nitamwinua juu.[q]

SURA 14

a Yos 24:7
b Zb 105:39
c Kut 14:16
Mdo 7:36
d Yos 2:10
Zb 66:6
Zb 106:9
Zb 114:3
Isa 51:10
e Ne 9:11
Zb 78:13
Zb 136:13
Isa 63:12
f Kut 15:19
Hes 33:8
Isa 63:13
1Ko 10:1
Ebr 11:29
g Kut 15:8
h Kut 14:17
Zb 10:2
i Kut 13:21
j Kut 23:27
1Sa 5:11
Zb 18:14
k Zb 76:6
l Kut 14:4
Kum 3:22
1Sa 4:8
m Kut 7:19
Kut 8:5

Safu ya 2

a Kut 15:1
b Kut 15:10
Kum 11:4
Ne 9:11
Zb 78:53
Ebr 11:29
c Mwa 15:14
Kut 14:23
Yos 24:7
d Kut 14:13
Zb 106:11
Zb 136:15
e Zb 66:6
Zb 77:19
f Kut 14:22
Kut 15:8
g Kum 4:20
Zb 106:8
h Zb 58:10
Zb 59:10
Zb 91:8
Met 16:4
i Kut 4:31
Kut 19:9
Zb 106:12

SURA 15

j Amu 5:1
2Sa 22:1
Ufu 15:3
k Kut 9:16
Kut 18:11
Zb 106:12
l Kut 15:21
Zb 136:15
m Kut 17:16
Zb 18:1
Isa 12:2
Flp 4:13
n Ufu 7:10
o 2Sa 22:47
Zb 99:5
Isa 25:1
p Kut 3:15
q Zb 83:18
Zb 148:13

3 Yehova ni mtu wa
vita[a] anayetenda kiume.
Yehova ndilo jina lake.[b]
4 Ametupa magari ya
Farao na majeshi yake
baharini.[c]
Na mashujaa wake wa
vita walio bora
wamezamishwa katika
Bahari Nyekundu.[d]
5 Maji yenye kututumuka
yaliwafunika;[e]
wakashuka ndani ya
vilindi kama jiwe.[f]
6 Mkono wako wa kuume,
Ee Yehova, unajionyesha
kuwa wenye nguvu
katika uwezo,[g]
Mkono wako wa kuume,
Ee Yehova, unaweza
kumvunja-vunja adui.[h]
7 Na katika wingi wa ukuu
wako wewe unaweza
kuwatupa chini wale
wanaosimama juu yako;[i]
Wewe unaituma hasira
yako inayowaka, nayo
inawateketeza kama
majani makavu.[j]
8 Na kwa pumzi
kutoka katika mianzi ya
pua[k] yako maji
yalirundamana;
Yalisimama tuli kama
bwawa la mafuriko;
Maji yenye kututumuka
yaligandamana katika
moyo wa bahari.
9 Adui alisema, 'Nitafuatilia!
Nitafikia![m]
Nitagawa nyara![n] Nafsi
yangu itajawa nazo!
Nitauchomoa upanga
wangu! Mkono wangu
utawafukuzia mbali!'[o]
10 Ulipuliza kwa pumzi yako,[p]
bahari ikawafunika;[q]
Walizama kama risasi
katika maji makuu.[r]

SURA 15

a Ne 4:20
Zb 24:8
b Kut 6:3
Isa 42:8
c Kut 14:27
Yos 24:6
d Kut 14:7
e Yos 24:7
f Ne 9:11
g Zb 17:7
Zb 60:5
Zb 89:13
Zb 118:15
1Pe 5:6
h Ebr 10:31
i Zb 148:13
Isa 5:16
Isa 37:23
j Kum 4:24
Zb 59:13
Ebr 12:29
k 2Sa 22:16
Zb 18:15
l Kut 14:8
m Kut 14:9
n Eze 38:12
o Kut 14:5
Isa 36:20
p Mwa 8:1
Kut 14:21
q Kut 14:28
Kum 11:4
r Kut 15:5
Ne 9:11

Safu ya 2

a Kum 3:24
2Sa 7:22
1Ko 8:5
b Law 19:2
Isa 6:3
1Pe 1:16
c Lu 12:5
Ebr 12:28
d Ebr 2:12
e Kut 11:9
f Kut 15:6
g Zb 78:53
Ebr 11:29
h Zb 106:10
i Zb 78:54
j Hes 14:14
Yos 2:10
k Zb 99:1
l Zb 48:6
m Hes 22:3
n Yos 2:11
Yos 5:1
o Kum 11:25
Yos 2:9
p Kut 19:5
Kum 32:9
2Sa 7:23
q Isa 43:1
r Hes 20:17
Hes 21:22
Kum 2:27
s Kum 4:21
Zb 44:2
Zb 78:54
Zb 80:8

11 Ni nani kati ya miungu
aliye kama wewe, Ee
Yehova?[a]
Ni nani aliye kama wewe,
unayejionyesha kuwa
mwenye nguvu katika
utakatifu?[b]
Unayestahili kuogopwa[c]
kwa nyimbo za sifa,[d]
Unayefanya mambo ya
ajabu.[e]
12 Uliunyoosha mkono wako
wa kuume,[f] nayo dunia
ikawameza.[g]
13 Wewe katika fadhili
zako zenye upendo
umewaongoza watu
ambao umewakomboa;[h]
Wewe katika nguvu zako
hakika utawaongoza
mpaka kwenye makao
yako matakatifu.[i]
14 Vikundi vya watu
vitasikia,[j] vitafadhaika;[k]
Uchungu wa kuzaa[l]
utawashika wakaaji wa
Ufilisti.
15 Wakati huo mashehe
wa Edomu kwa kweli
watasumbuka;
Nao wadhalimu wa Moabu,
kutetemeka
kutawashika.[m]
Wakaaji wote wa Kanaani
kwa kweli watavunjika
moyo.[n]
16 Woga na hofu zitaanguka
juu yao.[o]
Kwa sababu ya ukuu wa
mkono wako watatulia
kama jiwe,
Mpaka watu wako[p] wapite,
Ee Yehova,
Mpaka watu ambao
umewatokeza[q] wapite.[r]
17 Utawaleta na kuwapanda
katika mlima wa urithi
wako,[s]

Mahali palipofanywa imara
ambapo umetayarisha ili
ukae,[a] Ee Yehova,
Patakatifu,[b] Ee Yehova,
ambapo mikono yako
imepafanya imara.
18 Yehova atatawala akiwa
mfalme mpaka wakati
usio na kipimo, naam,
milele.[c]
19 Farasi wa Farao[d] pamoja na
magari yake ya vita na
askari wake
wapanda-farasi
walipoingia baharini,[e]
Ndipo Yehova
alipoyarudisha maji ya
bahari juu yao,[f]
Huku wana wa Israeli
wakitembea juu ya nchi
kavu katikati ya bahari."[g]
20 Naye Miriamu nabii, dada
ya Haruni,[h] akachukua tari
mkononi mwake;[i] na wanawa-
ke wote wakaanza kutoka pa-
moja naye wakiwa na matari na
kucheza dansi.[j] **21** Naye Miri-
amu akawa akiwaitikia wana-
ume:[k]
"Mwimbieni Yehova,[l] kwa
maana ametukuzwa
sana.[m]
Farasi na mpandaji wake
amewatupa baharini."[n]
22 Baadaye Musa akaondoa
Israeli kutoka katika Bahari
Nyekundu nao wakaenda
katika nyika ya Shuri[o] na ku-
piga mwendo kwa siku tatu nyi-
kani, lakini hawakupata maji.[p]
23 Mwishowe wakafika Mara,[q]
lakini hawakuweza kunywa
maji ya Mara kwa sababu yali-
kuwa machungu. Ndiyo sababu
alipaita jina Mara.[r] **24** Nao
watu wakaanza kunung'unika
juu ya Musa,[s] na kusema: "Tu-
takunywa nini?" **25** Kisha
yeye akamlilia Yehova.[t] Basi
Yehova akamwelekeza kwenye
mti fulani, naye akautupa nda-
ni ya maji nayo maji yakawa
matamu.[a]
Hapo Yeye akawawekea shar-
ti na kesi ya kuhukumia na
hapo akawatia katika jaribu.[b]
26 Naye akasema: "Ikiwa utai-
sikiliza kwa makini sauti ya Ye-
hova Mungu wako na kufanya
lililo sawa machoni pake na ku-
tega sikio usikie amri zake na
kushika masharti yake yote,[c] si-
taweka juu yako yoyote ya ma-
gonjwa yale niliyoweka juu ya
Wamisri;[d] kwa sababu mimi ni
Yehova anayekuponya."[e]
27 Baada ya hapo wakafika
Elimu, ambapo palikuwa na
mabubujiko 12 ya maji na mi-
tende 70.[f] Basi wakapiga kambi
hapo kando ya maji hayo.

16 Baadaye wakaondoka
Elimu,[g] nalo kusanyiko
zima la wana wa Israeli mwi-
showe likafika katika nyika ya
Sini,[h] iliyo katikati ya Elimu na
Sinai, siku ya kumi na tano ya
mwezi wa pili baada ya kuto-
ka kwao katika nchi ya Misri.
2 Nalo kusanyiko zima la
wana wa Israeli likaanza kunun-
g'unika juu ya Musa na Haru-
ni huko nyikani.[i] **3** Na wana
wa Israeli wakawa wakiwaam-
bia: "Laiti tungekufa[j] kwa
mkono wa Yehova katika nchi
ya Misri tulipokuwa tukike-
ti kando ya vyungu vya nya-
ma,[k] tulipokuwa tukila mkate
na kushiba, kwa sababu ninyi
mmetutoa na kutuleta nyika-
ni ili kuliua kutaniko lote kwa
njaa."[l]
4 Ndipo Yehova akamwa-
mbia Musa: "Tazama, nitawa-
nyeshea mkate kutoka mbingu-
ni;[m] nao watu watatoka nje na
kuokota kila mtu kiasi chake

SURA 15
a 1Fa 8:27
b Kut 25:8
c Zb 10:16
Zb 146:10
Da 4:3
d Kut 14:23
Met 21:31
e Yos 24:6
f Kut 14:28
Ebr 11:29
g Kut 14:22
h Hes 26:59
i Zb 81:2
j Amu 11:34
1Sa 18:6
2Sa 6:5
Zb 150:4
Yer 31:4
k 1Sa 18:7
l Amu 5:3
m Kut 14:17
Kut 18:11
n Kut 14:27
o Mwa 16:7
Mwa 25:18
p Kut 17:1
q Hes 33:8
r Ru 1:20
s Kut 16:2
Kut 17:3
Hes 11:1
1Ko 10:10
Yud 16
t Kut 17:4
Zb 50:15

Safu ya 2
a 2Fa 2:21
b Kut 16:4
Kum 8:2
1Pe 1:7
c Law 26:3
Kum 28:1
1Yo 5:3
d Kut 9:10
Kum 7:15
e Kut 23:25
Zb 103:3
f Hes 33:9

SURA 16
g Hes 33:10
h Hes 33:11
i Kut 15:24
Zb 106:25
1Ko 10:10
j Hes 14:2
Yon 4:8
k Hes 11:4
l Kut 17:3
Hes 16:13
Kum 8:3
Omb 4:9
m Zb 78:24
Zb 105:40
Yoh 6:31
1Ko 10:3

siku baada ya siku,[a] ili nipate
kuwajaribu iwapo watatembea
katika sheria yangu au hapana.[b] **5** Na itakuwa kwamba
katika siku ya sita[c] watatayarisha kile watakacholeta ndani,
nacho kitakuwa mara mbili ya
kile ambacho wao huokota siku
baada ya siku."[d]

6 Kwa hiyo Musa na Haruni wakawaambia wana wote wa
Israeli: "Wakati wa jioni hakika mtajua kwamba Yehova ndiye aliyewatoa ninyi katika nchi
ya Misri.[e] **7** Na asubuhi kwa
kweli mtauona utukufu wa Yehova,[f] kwa sababu amesikia
manung'uniko yenu juu ya Yehova. Na sisi ni nani hivi kwamba mnung'unike juu yetu?"
8 Naye Musa akaendelea kusema: "Itakuwa hivyo wakati
ambapo Yehova atawapa jioni
nyama ya kula na asubuhi mkate wa kuwashibisha, kwa sababu Yehova amesikia manung'uniko yenu mnayonung'unika
juu yake. Na sisi ni nani? Manung'uniko yenu si juu yetu, bali
ni juu ya Yehova."[g]

9 Naye Musa akamwambia
Haruni: "Liambie kusanyiko
zima la wana wa Israeli, 'Njooni
karibu mbele za Yehova, kwa sababu ameyasikia manung'uniko
yenu.'"[h] **10** Kisha ikawa kwamba mara tu baada ya Haruni
kusema na kusanyiko zima la
wana wa Israeli, wakageuka
na kutazama kuelekea nyikani,
na, tazama! utukufu wa Yehova
ukaonekana katika wingu.[i]

11 Naye Yehova akazidi kunena na Musa, na kusema:
12 "Nimeyasikia manung'uniko ya wana wa Israeli.[j] Sema
nao, na kuwaambia, 'Katikati
ya zile jioni mbili mtakula nyama na asubuhi mtashiba mkate;[a] nanyi hakika mtajua kwamba mimi ni Yehova Mungu
wenu.'"[b]

13 Basi ikawa kwamba wakati wa jioni kware[c] wakaanza kuja na kuifunika kambi,
na asubuhi kulikuwa kumetokea utando wa umande kuizunguka kambi.[d] **14** Baada ya
muda ule utando wa umande
ukawa mvuke, na tazama, juu
ya uso wa nyika kulikuwa na
kitu laini chenye chembechembe,[e] laini kama sakitu[f] juu ya
dunia. **15** Wana wa Israeli walipokiona, wakaanza kusemezana: "Ni nini hiki?" Kwa maana hawakujua kilikuwa nini.
Basi Musa akawaambia: "Ni
mkate ambao Yehova amewapa
ninyi uwe chakula.[g] **16** Hili
ndilo neno ambalo Yehova ameamuru, 'Okoteni kiasi chake,
kila mmoja kulingana na kiasi anachoweza kula. Mtachukua kipimo cha omeri[h] kwa ajili
ya kila mtu kulingana na hesabu ya nafsi ambazo kila mmoja
wenu anazo katika hema lake.'"
17 Nao wana wa Israeli wakaanza kufanya hivyo; nao wakakiokota, baadhi yao wakakusanya
kingi na wengine wakakusanya kichache. **18** Walipokipima kwa omeri, yule aliyekusanya kingi hakuwa na ziada na
yule aliyekusanya kichache hakuwa na upungufu.[i] Walikiokota kila mmoja kulingana na kiasi anachoweza kula.

19 Kisha Musa akawaambia:
"Mtu yeyote asiache chochote
mpaka asubuhi."[j] **20** Lakini
hawakumsikiliza Musa. Wakati ambapo watu fulani waliacha kiasi fulani mpaka asubuhi, kilitokeza wadudu na kunuka;[k] hivi kwamba Musa aliwakasirikia.[l] **21** Nao wakawa

SURA 16
a Ne 11:23
Met 30:8
Mt 6:11
b Kum 8:2
Yak 1:3
1Pe 1:7
c Kut 35:2
d Kut 16:22
e Kut 6:7
Hes 16:28
Zb 77:20
Isa 63:11
f Kut 24:10
Law 9:6
Hes 16:42
Yoh 11:40
g Hes 21:7
1Sa 8:7
Isa 32:6
Lu 10:16
h Kut 16:2
Hes 11:1
i Kut 13:21
Hes 16:19
1Fa 8:11
Mt 17:5
j Hes 14:27
Yud 16

Safu ya 2
a Zb 105:40
b Kut 4:5
Kut 6:7
Eze 34:31
c Hes 11:31
Zb 78:27
d Hes 11:9
e Hes 11:7
Kum 8:3
Ne 9:15
Zb 78:24
f Zb 147:16
g Hes 21:5
Kum 8:16
Yos 5:12
Yoh 6:31
Yoh 6:58
1Ko 10:3
Ebr 9:4
h Kut 16:36
i 2Ko 8:15
j Kut 12:10
Mt 6:34
k Mt 6:19
l Kut 32:19
Hes 16:15
Efe 4:26

wakikiokota asubuhi baada ya
asubuhi,[a] kila mmoja kulingana
na alichoweza kula. Jua lilipo-
kuwa kali, kiliyeyuka.
22 Na ikawa kwamba kati-
ka siku ya sita waliokota mara
mbili ya kiasi cha mkate,[b] vi-
pimo viwili vya omeri kwa kila
mtu. Kwa hiyo wakuu wote wa
kusanyiko wakaja na kumju-
lisha Musa. **23** Basi akawaam-
bia: "Ndivyo Yehova amesee-
ma. Kesho kutakuwa na kushi-
ka sabato, sabato takatifu kwa
Yehova.[c] Mnachoweza kuoka,
okeni, na mnachoweza kutoko-
sa, tokoseni,[d] na ziada yote ili-
yopo jiwekeeni akiba kiwe kitu
cha kuwekwa mpaka asubu-
hi." **24** Basi wakakiweka aki-
ba mpaka asubuhi, kama vile
Musa alivyokuwa ameamuru;
nacho hakikunuka wala fu-
nza hawakutokea ndani yake.[e]
25 Kisha Musa akasema: "Ku-
leni hiki leo, kwa sababu leo
ni sabato[f] kwa Yehova. Leo ha-
mtakipata uwanjani. **26** Siku
sita mtakiokota, lakini siku ya
saba ni sabato.[g] Siku hiyo ha-
kuna chochote kitakachofanyi-
zwa." **27** Hata hivyo, ikawa
kwamba katika siku ya saba ba-
adhi ya watu walitoka nje kwe-
nda kukiokota, lakini hawaku-
pata chochote.
28 Basi Yehova akamwa-
mbia Musa: "Ninyi watu mta-
endelea kukataa kushika amri
zangu na sheria zangu mpa-
ka wakati gani?[h] **29** Kumbu-
keni kwamba Yehova amewa-
pa ninyi sabato.[i] Ndiyo saba-
bu anawapa siku ya sita mkate
wa siku mbili. Endeleeni kukaa
kila mmoja mahali pake.[j] Mtu
yeyote asitoke mahali pake
siku ya saba." **30** Na watu wa-
kaishika sabato siku ya saba.[k]

SURA 16

a Mt 6:11
b Kut 16:5
c Kut 20:8
Kut 31:15
Kut 35:2
Law 23:3
Mk 2:27
d Hes 11:8
e Kut 16:33
f Ne 9:14
g Kut 20:9
Kut 31:13
Kum 5:15
Yer 17:22
Mt 12:12
Lu 13:15
h Hes 14:11
2Fa 17:14
Zb 78:10
Zb 81:13
Zb 106:13
Lu 16:31
i Kut 31:13
Isa 58:13
Eze 20:12
j Lu 23:56
k Law 23:3
Kum 5:14

Safu ya 2

a Kut 16:15
Hes 11:7
b Zb 105:5
Zb 111:4
c Zb 78:20
d Ebr 9:4
e Kut 27:21
Kut 30:6
Kut 40:20
1Fa 8:9
f Kum 8:2
Ne 9:21
Zb 78:24
Yoh 6:49
g Yos 5:12
Ne 9:15
h Hes 33:48
Kum 1:8
Kum 34:1

SURA 17

i Hes 33:12
j Hes 33:2
k Hes 33:14
l Kut 5:21
Hes 14:2
Hes 20:3
m Hes 14:22
Zb 78:18
Zb 95:9
Zb 106:14
Lu 4:12
1Ko 10:9
Ebr 3:9

31 Na nyumba ya Israeli ika-
anza kukiita jina lake "mana."
Nacho kilikuwa cheupe kama
mbegu za mgiligilani, na la-
dha yake ilikuwa kama ya keki
bapa zenye asali.[a] **32** Ki-
sha Musa akasema: "Hili ndi-
lo neno ambalo Yehova amea-
muru, 'Kijazeni kwenye kipimo
cha omeri kiwe kitu cha kuwe-
kwa katika vizazi vyenu vyo-
te,[b] ili wapate kuona mkate ni-
liowalisha ninyi nyikani nilipo-
kuwa nikiwatoa katika nchi ya
Misri.'"[c] **33** Kwa hiyo Musa
akamwambia Haruni: "Chu-
kua mtungi, uweke omeri moja
kamili ya mana na kuiweka
mbele za Yehova iwe kitu cha
kuwekwa katika vizazi vyenu
vyote."[d] **34** Sawasawa na vile
Yehova alivyokuwa amemwa-
muru Musa, Haruni akaiweka
mbele ya ule Ushuhuda[e] iwe
kitu cha kuwekwa. **35** Nao
wana wa Israeli wakala mana
miaka 40,[f] mpaka walipofika
katika nchi inayokaliwa.[g] Wa-
likula mana mpaka walipofi-
ka mpakani mwa nchi ya Kana-
ani.[h] **36** Omeri ni sehemu ya
kumi ya kipimo cha efa.

17 Nalo kusanyiko lote la
wana wa Israeli likaon-
doka katika nyika ya Sini[i] ha-
tua kwa hatua, kulingana na
agizo la Yehova,[j] nao wakapiga
kambi katika Refidimu.[k] Lakini
hapakuwa na maji ya kunywa
kwa ajili ya watu.
2 Na watu wakaanza kugo-
mbana na Musa na kusema:[l]
"Tupe maji tunywe." Lakini
Musa akawaambia: "Kwa nini
mnagombana na mimi? Kwa
nini mnaendelea kumjaribu
Yehova?"[m] **3** Na watu wakae-
ndelea kuwa na kiu ya maji
wakiwa huko, na watu waka-

endelea kunung'unika juu ya
Musa na kusema: "Kwa nini
umetutoa Misri ili kutuua kwa
kiu sisi na wana wetu na mifu-
go yetu?"[a] **4** Mwishowe Musa
akamlilia Yehova, na kusema:
"Nitafanya nini na watu hawa?
Bado muda kidogo nao watani-
piga kwa mawe!"[b]

5 Kisha Yehova akamwa-
mbia Musa: "Pita mbele ya
watu[c] na uchukue pamoja nawe
baadhi ya wanaume wazee wa
Israeli na fimbo yako amba-
yo uliitumia kupiga maji ya
Mto Nile.[d] Ichukue mkononi
mwako nawe uendelee kute-
mbea. **6** Tazama! Nitasima-
ma mbele yako juu ya mwamba
huko Horebu. Nawe utaupiga
mwamba huo, na maji yatato-
ka ndani yake, na watu watay-
anywa."[e] Kisha Musa akafanya
hivyo machoni pa wanaume wa-
zee wa Israeli. **7** Basi akapai-
ta mahali hapo jina Masa[f] na
Meriba,[g] kwa sababu ya kugo-
mbana kwa wana wa Israe-
li na kwa sababu ya kumjari-
bu Yehova,[h] na kusema: "Je, Ye-
hova yuko katikati yetu au ha-
pana?"[i]

8 Nao Waamaleki[j] wakaja na
kupigana na Israeli huko Re-
fidimu.[k] **9** Ndipo Musa aka-
mwambia Yoshua:[l] "Tuchagulie
wanaume, nawe uende[m] ukapi-
gane na Waamaleki. Kesho ni-
tasimama juu ya kilima, niki-
wa na fimbo ya Mungu wa kwe-
li mkononi mwangu."[n] **10** Ki-
sha Yoshua akafanya kama
vile Musa alivyokuwa ame-
mwambia,[o] ili kupigana na Wa-
amaleki; na Musa, Haruni na
Huru[p] wakapanda mpaka juu
ya kilima.

11 Na ikawa kwamba mara
tu Musa alipoinua mkono wake
juu, Waisraeli wakawa na ngu-
vu zaidi;[a] lakini mara tu ali-
poushusha mkono wake, Waa-
maleki wakawa na nguvu zaidi.
12 Mikono ya Musa ilipokuwa
mizito, walichukua jiwe wakali-
weka chini yake, naye akalika-
lia; naye Haruni na Huru waka-
itegemeza mikono yake, mmoja
upande huu na yule mwingine
upande ule, hivi kwamba mi-
kono yake ikawa imara mpaka
jua lilipotua. **13** Basi Yoshua
akawashinda kabisa Amaleki
na watu wake kwa makali ya
upanga.[b]

14 Sasa Yehova akamwa-
mbia Musa: "Andika hili kati-
ka kitabu[c] liwe ukumbusho na
uliseme masikioni mwa Yoshua,
'Nitafutilia mbali kabisa ukum-
busho wa Amaleki toka chini
ya mbingu.'"[d] **15** Naye Musa
akajenga madhabahu na kuii-
ta jina Yehova-nisi, **16** na ku-
sema: "Kwa sababu kuna mko-
no dhidi ya kiti cha ufalme[e] cha
Yah,[f] Yehova atakuwa na vita
na Amaleki kizazi baada ya ki-
zazi."[g]

18 Sasa Yethro kuhani wa
Midiani, baba-mkwe wa
Musa,[h] akasikia mambo yote
ambayo Mungu alikuwa ameya-
fanya kwa ajili ya Musa na kwa
ajili ya Israeli watu wake, jinsi
Yehova alivyokuwa amewatoa
Israeli kutoka Misri.[i] **2** Basi
Yethro, baba-mkwe wa Musa,
akamchukua Sipora, mke wa
Musa, baada ya kuachwa aende
zake, **3** na wanawe wawili,[j]
ambao jina la mmoja wao liliku-
wa Gershomu,[k] "kwa sababu,"
akasema, "nimekuwa mkaaji
mgeni katika nchi ya kigeni";
4 nalo jina la yule mwingine li-
likuwa Eliezeri,[l] "kwa sababu,"
kama alivyosema, "Mungu wa
baba yangu ni msaidizi wangu

SURA 17
a Kut 16:2
b 1Sa 30:6
Yoh 10:31
c Eze 2:6
d Kut 7:20
e Hes 20:8
Kum 8:15
Ne 9:15
Zb 78:15
Zb 105:41
Zb 114:8
Isa 48:21
1Ko 10:4
f Kum 9:22
Kum 33:8
g Zb 81:7
h Kum 6:16
Zb 95:8
Ebr 3:8
i Kut 34:9
Kum 31:17
Mdo 7:39
j Mwa 36:12
k Kum 25:17
1Sa 15:2
l Hes 11:28
Kum 32:44
Mdo 7:45
m Hes 31:3
n Kut 4:2
o Yos 11:15
p Kut 24:14

Safu ya 2
a Zb 56:9
b Yos 11:12
c Kut 34:27
d Hes 24:20
Kum 25:19
1Nya 4:43
e Isa 66:1
Mdo 7:49
f Zb 94:12
Isa 12:2
Isa 26:4
Ufu 19:1
g 1Sa 15:20
Est 3:1
Est 7:10
Est 9:24

SURA 18
h Kut 2:21
Kut 3:1
i Yos 2:10
Yos 9:9
j Mdo 7:29
k Kut 2:22
l 1Nya 23:15

kwa kuwa alinikomboa kutokana na upanga wa Farao."[a]

5 Basi Yethro, baba-mkwe wa Musa, pamoja na wanawe na mke wake wakamjia Musa huko nyikani ambako alikuwa amepiga kambi, kwenye mlima wa Mungu wa kweli.[b] **6** Kisha akatuma neno kwa Musa: "Mimi, baba-mkwe wako, Yethro,[c] nimekuja kwako, na pia mke wako na wanawe wawili pamoja naye." **7** Mara moja Musa akatoka kwenda kumpokea baba-mkwe wake, naye akajilaza kifudifudi mbele yake na kumbusu;[d] na kila mmoja wao akaanza kuuliza jinsi yule mwingine alivyokuwa akiendelea. Kisha wakaingia hemani.

8 Naye Musa akaanza kumsimulia baba-mkwe wake yote ambayo Yehova alikuwa amemtendea Farao na Misri kwa sababu ya Israeli,[e] na magumu yote yaliyokuwa yamewapata njiani,[f] na bado Yehova alikuwa akiwakomboa.[g] **9** Kisha Yethro akawa na furaha kwa sababu ya mema yote ambayo Yehova alikuwa ametenda kwa ajili ya Israeli kwa kuwa alikuwa amewakomboa kutoka katika mkono wa Misri.[h] **10** Basi Yethro akasema: "Na abarikiwe Yehova, ambaye amewakomboa kutoka katika mkono wa Misri na kutoka katika mkono wa Farao, na ambaye amewakomboa watu kutoka katika mkono wa Misri.[i] **11** Sasa najua kwamba Yehova ni mkuu kuliko miungu[j] mingine yote kwa sababu ya jambo hili walilotenda kwa kimbelembele dhidi yao." **12** Kisha Yethro, baba-mkwe wa Musa, akachukua toleo la kuteketezwa na dhabihu kwa ajili ya Mungu;[k] naye Haruni na wanaume wote wazee wa Israeli wakaja kula mkate pamoja na baba-mkwe wa Musa, mbele za Mungu wa kweli.[a]

13 Na ikawa kwamba siku iliyofuata, Musa akaketi chini kama kawaida ili ahukumu watu,[b] nao watu wakasimama mbele ya Musa tangu asubuhi mpaka jioni. **14** Naye baba-mkwe wa Musa akaona yote aliyokuwa akiyatenda kwa ajili ya watu. Basi akasema: "Ni shughuli ya aina gani hii unayotenda kwa ajili ya watu? Kwa nini ni wewe peke yako unayeendelea kuketi, na watu wote wanaendelea kusimama mbele yako tangu asubuhi mpaka jioni?" **15** Ndipo Musa akamwambia baba-mkwe wake: "Kwa sababu watu huendelea kunijia ili kuuliza habari kutoka kwa Mungu.[c] **16** Ikitokea kwamba wana kesi ambayo imezuka,[d] hiyo lazima ije kwangu, nami lazima niamue kati ya upande mmoja na ule mwingine, nami lazima nijulishe maamuzi ya Mungu wa kweli na sheria zake."[e]

17 Ndipo baba-mkwe wa Musa akamwambia: "Si vema jinsi unavyofanya. **18** Utachoka, wewe na watu hawa walio pamoja nawe, kwa sababu shughuli hii ni mzigo mkubwa mno kwako.[f] Wewe huwezi kuifanya peke yako.[g] **19** Sasa sikiliza sauti yangu.[h] Nitakushauri, na Mungu atakuwa pamoja nawe.[i] Wewe mwenyewe uwe mwakilishi kwa ajili ya watu mbele za Mungu wa kweli,[j] na wewe mwenyewe utaleta kesi hizo mbele za Mungu wa kweli.[k] **20** Nawe utawaonya juu ya masharti na sheria,[l] nawe utawajulisha njia wanayopaswa kuitembea na kazi wana-

SURA 18

a Kut 2:15
2Ko 1:10
b Kut 19:2
1Fa 19:8
c Kut 4:18
Hes 10:29
d Mwa 33:3
2Sa 14:33
Ro 12:10
e Kut 7:3
Kut 14:28
Kum 4:34
Ne 9:10
f Kut 15:22
Kut 16:3
Hes 20:14
g Zb 81:7
Zb 102:2
Da 3:29
h Kum 33:29
Ro 15:10
i Mwa 14:20
Lu 1:68
j Kut 15:11
2Nya 2:5
Zb 95:3
Zb 97:9
Da 2:47
k Mal 1:11

Safu ya 2

a Mwa 31:54
b Mt 23:2
c Kut 20:19
Hes 12:8
Hes 27:5
d Kut 24:14
Kum 17:8
1Ko 6:1
e Kum 4:5
Kum 5:1
Kum 6:1
f Hes 11:11
g Hes 11:14
Kum 1:9
Mdo 6:2
h Kut 18:24
Met 9:9
i Yos 1:17
j Kut 20:19
Kum 5:5
k Hes 27:5
l Kum 7:11
Ne 9:14
Mk 10:3

yopaswa kuifanya.[a] **21** Lakini wewe mwenyewe unapaswa
kuchagua kutoka kati ya watu
wote wanaume wenye uwezo,[b]
wanaomwogopa Mungu,[c] wana-
ume wenye kutegemeka,[d] wa-
naochukia faida isiyo ya haki;[e]
na lazima uwaweke hao juu yao
wawe wakuu juu ya maelfu,[f]
wakuu juu ya mamia, wakuu
juu ya 50, na wakuu juu ya ma-
kumi.[g] **22** Nao watawahuku-
mu watu kwenye kila pindi ina-
yofaa; na itakuwa kwamba kila
kesi kubwa watakuletea wewe,[h]
lakini kila kesi ndogo wao we-
nyewe wataishughulikia waki-
wa waamuzi. Kwa hiyo jirahi-
sishie mambo, nao wataubeba
mzigo pamoja nawe.[i] **23** Uki-
fanya jambo hilo hasa, naye
Mungu amekuamuru, hapo ndi-
po hakika utakapoweza kuli-
stahimili na, zaidi ya hilo, watu
hawa wataenda mahali pao we-
nyewe kwa amani."[j]

24 Musa akaisikiliza sauti ya
baba-mkwe wake mara moja na
kufanya yote aliyokuwa amese-
ma.[k] **25** Naye Musa akacha-
gua wanaume wenye uwezo
kutoka Israeli lote na kuwa-
pa vyeo vya kuwa vichwa juu
ya watu,[l] kuwa wakuu wa ma-
elfu, wakuu wa mamia, wa-
kuu wa 50 na wakuu wa maku-
mi. **26** Nao wakawahukumu
watu katika kila pindi inayo-
faa. Kesi ngumu walikuwa wa-
kimletea Musa,[m] lakini kila
kesi ndogo wao wenyewe wali-
ishughulikia wakiwa waamuzi.
27 Kisha Musa akamsindikiza
baba-mkwe wake,[n] naye akaen-
da zake kwenye nchi yake.

19 Katika mwezi wa tatu
baada ya wana wa Israe-
li kutoka katika nchi ya Mi-
sri,[o] siku hiyo hiyo, wakaingia
katika nyika ya Sinai.[a] **2** Nao
wakaanza safari kutoka Refi-
dimu,[b] wakaingia katika nyika
ya Sinai, wakapiga kambi nyi-
kani;[c] nao Israeli wakapiga ka-
mbi hapo mbele ya mlima.[d]

3 Naye Musa akapanda kwe-
nda kwa Mungu wa kweli, na
Yehova akaanza kumwita toka
mlimani,[e] na kusema: "Hivi ndi-
vyo utakavyoiambia nyumba
ya Yakobo na kuwaambia wana
wa Israeli, **4** 'Ninyi wenyewe
mmeona niliyowatendea Wami-
sri,[f] ili nipate kuwachukua ni-
nyi juu ya mabawa ya tai na
kuwaleta kwangu.[g] **5** Na sasa
ikiwa mtaitii[h] sauti yangu kabi-
sa na kulishika kwa kweli aga-
no[i] langu, ndipo hakika mtaka-
pokuwa mali yangu ya pekee
kutoka kati ya vikundi vingi-
ne vyote vya watu,[j] kwa sababu
dunia nzima ni yangu.[k] **6** Na
ninyi wenyewe mtakuwa kwa-
ngu ufalme wa makuhani na ta-
ifa takatifu.'[l] Hayo ndiyo mane-
no utakayowaambia wana wa
Israeli."

7 Basi Musa akaja na kuwa-
ita wanaume wote wazee[m]
kati ya watu na kuweka mbele
yao maneno hayo yote ambayo
Yehova alikuwa amemwamu-
ru.[n] **8** Kisha watu wote waka-
jibu kwa pamoja na kusema:
"Yote ambayo Yehova amesema
tuko tayari kuyafanya."[o] Mara
moja Musa akarudi na kumwa-
mbia Yehova maneno ya watu.[p]
9 Ndipo Yehova akamwambia
Musa: "Tazama! Nitakujia kati-
ka wingu lenye giza,[q] ili watu
wapate kusikia ninaposema
nawe,[r] ili wapate kukuamini
wewe pia mpaka wakati usio
na kipimo."[s] Kisha Musa aka-
mwambia Yehova maneno ya
watu.

SURA 18

a 1Sa 12:23
Zb 32:8
Isa 30:21
Yer 42:3
Mik 4:2
b Hes 11:17
Kum 1:13
Mdo 6:3
1Ti 3:2
Tit 1:9
c 2Nya 6:31
2Nya 19:7
Ayu 2:3
Met 8:13
d Eze 18:8
Da 6:5
1Th 2:10
1Ti 3:7
Tit 1:7
e Kut 23:8
Mdo 20:33
1Ti 3:3
1Pe 5:2
f Hes 10:4
g Kum 1:15
Mdo 14:23
Tit 1:5
h Law 24:11
Hes 15:33
Kum 1:17
i Hes 11:17
j Met 11:14
k Met 12:15
l Mdo 6:5
m Mdo 15:2
n Hes 10:29

SURA 19

o Est 8:9

Safu ya 2

a Law 7:38
b Kut 17:1
c Hes 33:15
d Kut 3:12
e Ne 9:13
Mdo 7:38
f Kum 4:34
g Kum 32:11
Isa 63:9
h Zb 119:4
Met 19:16
1Yo 5:3
i 1Fa 8:21
Zb 25:10
Ga 4:24
j 1Fa 8:53
Zb 135:4
k Kum 10:14
1Ko 10:26
l Law 11:44
Kum 7:6
Isa 61:6
1Pe 2:9
Ufu 5:10
m Kut 3:16
n Kut 24:3
o Kut 24:7
Kum 26:17
Yos 24:24
p Hes 12:8
q Kum 4:11
1Fa 8:12
Zb 97:2
Ebr 12:18
r Kum 4:12
Kum 4:36
Mdo 7:38
s Lu 10:16

10 Na Yehova akaendelea kumwambia Musa: “Nenda kwa watu, ukawatakase leo na kesho, nao wafue nguo zao za kujitanda.[a] **11** Na wawe tayari kwa ajili ya siku ya tatu, kwa sababu katika siku ya tatu Yehova atashuka chini mbele ya macho ya watu wote juu ya Mlima Sinai.[b] **12** Nawe uwawekee watu mipaka pande zote, na kusema, ‘Jihadharini juu ya kupanda mlimani, wala msiguse ukingo wake. Mtu yeyote atakayeugusa mlima hakika atauawa.[c] **13** Mkono wowote usimguse, kwa maana lazima atapigwa kwa mawe au kwa mshale. Iwe ni mnyama au mwanadamu, hataishi.’[d] Pembe ya kondoo[e] itakapopigwa wao wenyewe wanaweza kuja mpaka kwenye mlima.”

14 Kisha Musa akateremka kutoka mlimani, akawaendea watu, naye akaanza kuwatakasa watu; nao wakaanza kufua nguo zao za kujitanda.[f] **15** Kwa hiyo akawaambia watu: “Jitayarisheni[g] siku hizi tatu. Ninyi wanaume msimkaribie mwanamke.”[h]

16 Na katika siku ya tatu kulipokuwa asubuhi, mingurumo na umeme zikaanza kutokea,[i] na wingu zito[j] juu ya mlima na sauti kubwa sana ya pembe,[k] hivi kwamba watu wote waliokuwa kambini wakaanza kutetemeka.[l] **17** Basi Musa akawatoa watu nje ya kambi ili wakutane na Mungu wa kweli, nao wakasimama kwenye sehemu ya chini ya mlima.[m] **18** Nao Mlima Sinai ukatoa moshi kila mahali,[n] kwa kuwa Yehova alikuwa ameshuka juu yake katika moto;[o] na moshi wake ukawa ukipaa kama moshi wa tanuru,[p] na mlima wote ulikuwa ukitetemeka sana.[a] **19** Sauti ya pembe ilipozidi kuwa kubwa, Musa akaanza kusema, naye Mungu wa kweli akaanza kumjibu kwa sauti.[b]

20 Basi Yehova akashuka chini kwenye Mlima Sinai, juu ya kilele cha mlima. Kisha Yehova akamwita Musa aje kwenye kilele cha mlima, naye Musa akaenda juu.[c] **21** Sasa Yehova akamwambia Musa: “Shuka, uwaonye watu, wasijaribu kupenya kwa Yehova ili kumwona na wengi wao walazimike kuanguka.[d] **22** Nao makuhani pia ambao humkaribia Yehova kwa ukawaida wajitakase,[e] ili Yehova asilipuke juu yao.”[f] **23** Ndipo Musa akamwambia Yehova: “Watu hawawezi kuja kwenye Mlima Sinai, kwa sababu wewe mwenyewe tayari ulituonya, na kusema, ‘Wekeni mipaka kwa ajili ya mlima na kuufanya kuwa mtakatifu.’”[g] **24** Hata hivyo, Yehova akamwambia: “Nenda, teremka, nawe uje juu, wewe na Haruni pamoja nawe; bali usiache makuhani na watu wapenye na kuja kwa Yehova, ili asije akalipuka juu yao.”[h] **25** Basi Musa akateremka kwa watu na kuwaambia.[i]

20 Na Mungu akaanza kunena maneno haya yote, na kusema:[j]

2 “Mimi ni Yehova Mungu wako,[k] ambaye nimekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya watumwa.[l] **3** Usiwe na miungu mingine[m] yoyote dhidi ya uso wangu.

4 “Usijifanyie sanamu ya kuchongwa wala umbo lililo kama kitu chochote kilicho juu mbinguni wala kilicho chini duniani wala kilicho ndani ya maji

SURA 19
a Hes 8:21
b Kut 34:5
Kum 33:2
Zb 18:9
c Law 10:2
2Sa 6:7
d Ebr 12:20
e Kut 20:18
Yos 6:4
f Kut 19:10
Yos 7:13
1Sa 16:5
g Amo 4:12
h 1Sa 21:4
1Ko 7:5
i Zb 77:18
j Kum 4:11
1Fa 8:12
Zb 97:2
k Ebr 12:19
l Ebr 12:21
m Kum 4:10
Kum 5:5
n Kum 4:11
Kum 5:22
Zb 68:8
Zb 104:32
o Kut 24:17
2Nya 7:3
p Mwa 19:28
Zb 144:5

Safu ya 2
a 1Fa 19:11
Zb 68:8
b Ne 9:13
Zb 81:7
c Kut 24:12
d 1Sa 6:19
e Kut 28:41
f Law 10:2
1Nya 13:10
Mdo 5:5
g Kut 19:12
h Hes 16:35
i Mdo 20:27

SURA 20
j Kum 5:22
Mdo 7:38
k Zb 81:10
Ho 13:4
Ro 3:29
l Kut 13:3
m Kum 5:7
2Fa 17:35
Yer 25:6

chini ya dunia.[a] **5** Usiviinamie wala kushawishiwa kuvitumikia,[b] kwa sababu mimi Yehova Mungu wako ni Mungu anayetaka watu wajitoe kikamili,[c] na ambaye huleta adhabu juu ya wana kwa sababu ya kosa la akina baba, juu ya kizazi cha tatu na juu ya kizazi cha nne, kwa wale wanaonichukia;[d] **6** lakini huonyesha fadhili zenye upendo kuelekea kizazi cha elfu kwa wale wanaonipenda na kuzishika amri zangu.[e]

7 "Usilitumie jina la Yehova Mungu wako kwa njia isiyofaa,[f] kwa maana Yehova hatamwacha bila kuadhibiwa yule anayelitumia jina lake kwa njia isiyofaa.[g]

8 "Kwa kuikumbuka siku ya sabato ili kuiona kuwa takatifu,[h] **9** utafanya utumishi nawe uifanye kazi yako yote kwa siku sita.[i] **10** Lakini siku ya saba ni sabato kwa Yehova Mungu wako.[j] Usifanye kazi yoyote, wewe wala mwana wako wala binti yako, mtumwa wako wala kijakazi wako wala mnyama wako wa kufugwa wala mgeni wako aliye ndani ya malango yako.[k] **11** Kwa maana katika siku sita Yehova alizifanya mbingu na dunia, bahari na kila kilichomo,[l] naye akaanza kupumzika siku ya saba.[m] Ndiyo sababu Yehova aliibariki siku ya sabato na kuifanya kuwa takatifu.[n]

12 "Mheshimu baba yako na mama yako[o] ili siku zako zipate kuwa ndefu juu ya nchi ambayo Yehova Mungu wako anakupa wewe.[p]

13 "Usiue.[q]

14 "Usifanye uzinzi.[r]

15 "Usiibe.[s]

16 "Usishuhudie kwa uwongo ukiwa shahidi dhidi ya mwenzako.[a]

17 "Usiitamani nyumba ya mwenzako. Usimtamani mke wa mwenzako,[b] wala mtumwa wake wala kijakazi wake wala ng'ombe-dume wake wala punda wake wala chochote cha mwenzako."[c]

18 Sasa watu wote walikuwa wakiona ile mingurumo na miwako ya umeme na sauti ya baragumu na mlima ukitoa moshi. Watu walipoona hilo, ndipo wakatetemeka na kusimama mbali.[d] **19** Nao wakaanza kumwambia Musa: "Wewe sema nasi, nasi tusikie; lakini Mungu asiseme nasi tusije tukafa."[e] **20** Basi Musa akawaambia watu: "Msiogope, kwa sababu Mungu wa kweli amekuja ili kuwatia ninyi katika jaribu,[f] na ili kumwogopa yeye, kuendelee kuwa mbele ya nyuso zenu ili ninyi msije mkatenda dhambi."[g] **21** Na watu wakaendelea kusimama mbali, bali Musa akaenda karibu na lile wingu kubwa jeusi mahali alipokuwa Mungu wa kweli.[h]

22 Naye Yehova akaendelea kumwambia Musa:[i] "Hivi ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli, 'Ninyi wenyewe mmeona kwamba nilisema nanyi kutoka mbinguni.[j] **23** Msifanye miungu ya fedha pamoja nami, wala msijifanyie miungu ya dhahabu.[k] **24** Utanifanyia madhabahu ya udongo,[l] nawe utatoa juu yake dhabihu za matoleo yako ya kuteketezwa na dhabihu zako za ushirika, kundi lako na mifugo yako.[m] Katika kila mahali ambapo nitalifanya

SURA 20

a Law 26:1; Kum 4:16; Kum 5:8; Isa 40:25; Mdo 17:29; 1Ko 8:4; Ufu 9:20
b Mwa 35:2; Kut 23:24; 1Ko 10:20; 1Yo 5:21
c Kut 34:14; Hes 25:11; Mt 4:10; Lu 10:27
d Kum 5:9; 2Sa 21:6; 1Fa 21:29; Mt 23:35
e Kum 4:37; Kum 5:10; Mhu 12:13; Ro 11:28
f Law 19:12; Met 30:9; Eze 36:21
g Law 24:16; Kum 5:11; Yos 9:20
h Kut 16:23; Kut 31:13; Kum 5:12
i Kut 23:12; Kum 5:13; Lu 13:14
j Kut 34:21
k Kut 16:29; Kum 5:14; Ne 13:16; Yoh 7:23
l Mdo 4:24; Mdo 14:15; Ufu 10:6; Ufu 14:7
m Mwa 2:2; Ebr 4:4
n Kum 5:12
o Kut 21:15; Met 1:8; Yer 35:18
p Law 19:3; Kum 5:16; Mt 15:4; Efe 6:2
q Mwa 9:6; Kum 5:17; Yak 2:11; 1Yo 3:15; Ufu 21:8
r Mwa 39:9; Kum 5:18; Met 6:32; Mt 5:27; Mt 5:28; Ro 13:9; 1Ko 6:18; Ebr 13:4
s Law 19:11; Kum 5:19; Mk 10:19; 1Ko 6:10; Efe 4:28

Safu ya 2

a Law 19:16; Kum 5:20; Kum 19:16; Zb 15:3
b Mt 5:28
c Yos 7:21; Mik 2:2; Lu 12:15; Ro 7:7
d Kut 19:16; Ebr 12:18
e Kum 18:16; Mdo 7:38; Ga 3:19

f Mwa 22:1; Kum 8:2; g Yos 24:14; Ayu 28:28; Met 1:7; Isa 8:13; h Kum 5:5; Zb 97:2; i Kut 33:1; Hes 12:8; j Kum 4:36; Ne 9:13; k Kut 32:4; Da 5:4; Mdo 17:29; l 2Fa 5:17; m Law 6:9; Ayu 1:5.

jina langu likumbukwe nitakuja kwako, nami hakika nitakubariki.[a] **25** Na ikiwa utanifanyia madhabahu ya mawe, usiijenge kwa mawe yaliyochongwa. Ikiwa utatumia tindo juu yake, basi utaitia unajisi.[b] **26** Nawe usipande juu ya madhabahu yangu kwa ngazi, ili sehemu zako za siri zisifunuliwe juu yake.'

21 "Nayo haya ndiyo maamuzi ya hukumu utakayoweka mbele yao:[c]

2 "Ikiwa utamnunua mtumwa[d] Mwebrania, atakuwa mtumwa kwa miaka sita, lakini mwaka wa saba ataondoka kama mtu aliyewekwa huru bila malipo.[e] **3** Ikiwa ataingia akiwa peke yake, ataondoka akiwa peke yake. Ikiwa ana mke, basi mke wake ataondoka pamoja naye. **4** Ikiwa bwana wake atampa mke, naye amzalie wana na mabinti, huyo mke na watoto wake watakuwa wa bwana wake[f] naye ataondoka akiwa peke yake.[g] **5** Lakini ikiwa mtumwa huyo atasisitiza kusema, 'Nampenda bwana wangu kwelikweli, mke wangu na wanangu; sitaki kuondoka kama mtu aliyewekwa huru,'[h] **6** basi bwana wake atamleta karibu na Mungu wa kweli naye atamleta kwenye mlango au kwenye mwimo wa mlango; naye bwana wake atalichoma sikio lake na kulitoboa kwa sindano, naye atakuwa mtumwa wake mpaka wakati usio na kipimo.[i]

7 "Ikiwa mtu atamuuza binti yake awe kijakazi,[j] hataondoka kama vile wanaume watumwa wanavyoondoka. **8** Ikiwa hapendezi machoni pa bwana wake hivi kwamba hamfanyi kuwa suria[k] bali anamfanya akombolewe, hatakuwa na haki ya kumuuza kwa watu wa kigeni katika kumtendea kwake kwa hila. **9** Na ikiwa atamfanya awe wa mwana wake, atamtendea kulingana na haki wanazostahili mabinti.[a] **10** Ikiwa atajichukulia mke mwingine, chakula chake, mavazi yake[b] na haki yake ya ndoa[c] hazitapunguzwa. **11** Ikiwa hatampa mambo hayo matatu, basi kijakazi huyo ataondoka bure, bila kulipa pesa.

12 "Yule anayempiga mtu na kumuua lazima atauawa.[d] **13** Lakini ikiwa mtu hakuvizia naye Mungu wa kweli aruhusu jambo hilo litokee mkononi mwake,[e] basi nitakuwekea mahali anapoweza kukimbilia.[f] **14** Na ikiwa mtu atawaka hasira juu ya mwenzake kufikia hatua ya kumuua kwa kutumia hila,[g] utamwondoa hata kwenye madhabahu yangu akafe.[h] **15** Naye anayempiga baba yake na mama yake lazima auawe.[i]

16 "Naye anayemteka nyara mtu[j] na kumuuza[k] au ambaye mikononi mwake huyo aliyetekwa amepatikana lazima auawe.[l]

17 "Naye anayemlaani baba yake na mama yake lazima atauawa.[m]

18 "Na watu wakianza ugomvi na mmoja wao ampige mwenzake kwa jiwe au jembe naye asife bali alazimike kuendelea kukaa kitandani mwake; **19** ikiwa atasimama na kutembea nje ya milango kwa kitu fulani cha kumtegemeza, basi yule aliyempiga hatapata adhabu; atalipa kwa ajili tu ya wakati uliopotea wa mtu huyo wa kufanya kazi mpaka awe amepona kabisa.

SURA 20
a Kum 12:5
2Nya 6:6
b Kum 27:5
Yos 8:31

SURA 21
c Kut 24:3
Kum 4:14
Ufu 15:4
d Law 25:39
2Fa 4:1
Mt 18:25
e Kum 15:12
Yer 34:14
f Law 25:44
Law 25:46
g Kum 15:12
h Kum 15:16
i Kum 15:17
j Ne 5:5
k Mwa 16:5
Ga 4:22

Safu ya 2
a Hes 30:16
b Efe 5:29
1Ti 5:8
c Kum 25:5
1Ko 7:3
d Mwa 9:6
Hes 35:30
Mt 5:21
e Hes 35:22
Kum 19:4
Mhu 9:11
f Hes 35:11
Kum 4:42
Kum 19:3
Yos 20:7
g Hes 15:30
Kum 19:11
2Sa 3:27
1Yo 3:15
h 1Fa 1:50
1Fa 2:29
2Fa 11:15
i Kut 20:12
1Ti 1:9
j Mwa 40:15
1Ti 1:10
k Mwa 37:28
l Kum 24:7
m Law 20:9
Met 20:20
Met 30:11
Met 30:17
Mt 15:4

20 "Na ikiwa mtu atampiga[a] mtumwa wake au kijakazi wake kwa fimbo naye kwa kweli afe chini ya mkono wake, lazima huyo atalipizwa kisasi.[b] **21** Hata hivyo, akikaa kwa siku moja au siku mbili, hatalipizwa kisasi, kwa sababu yeye ni pesa zake.

22 "Na ikiwa watu watapambana nao kwa kweli wamuumize sana mwanamke mwenye mimba nao watoto[c] wake watoke lakini kifo kisitokee, atadaiwa alipie hasara kulingana na kile ambacho mume wa mwanamke huyo atamdai; naye atakitoa kupitia kwa waamuzi.[d] **23** Lakini kifo kikitokea, basi utatoa nafsi kwa nafsi,[e] **24** jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu,[f] **25** alama kwa alama, jeraha kwa jeraha, pigo kwa pigo.[g]

26 "Na ikiwa mtu atalipiga jicho la mtumwa wake au jicho la kijakazi wake na kwa kweli aliharibu vibaya, atamwacha aende zake kama mtu aliyewekwa huru ili kulipia jicho lake.[h] **27** Na ikiwa ni jino la mtumwa wake au jino la kijakazi wake ndilo ameng'oa, atamwacha aende zake kama mtu aliyewekwa huru ili kulipia jino lake.

28 "Na ikiwa ng'ombe-dume atampiga kwa pembe mwanamume au mwanamke naye afe, lazima ng'ombe-dume huyo atapigwa kwa mawe,[i] lakini nyama yake isiliwe; na mwenye ng'ombe-dume huyo hatapata adhabu. **29** Lakini ikiwa ng'ombe-dume huyo alikuwa na zoea la kupiga kwa pembe tangu zamani na mwenye ng'ombe-dume huyo alionywa bali hakumzuia, naye amuue mwanamume au mwanamke, ng'ombe-dume huyo atapigwa kwa mawe na pia mwenye ng'ombe-dume huyo atauawa. **30** Ikiwa atadaiwa fidia, basi atatoa bei ya ukombozi kwa ajili ya nafsi yake kulingana na yote atakayodaiwa.[a] **31** Ikiwa ng'ombe-dume huyo alimpiga mwana au alimpiga binti, mwenye ng'ombe-dume atatendewa kulingana na uamuzi huu wa hukumu.[b] **32** Ikiwa aliyepigwa ni mtumwa au ni kijakazi, mwenye ng'ombe-dume atamlipa bwana wake bei ya shekeli 30,[c] naye ng'ombe-dume atapigwa kwa mawe.

33 "Na mtu akifunua shimo, au mtu akichimba shimo naye asilifunike, na ng'ombe-dume au punda aanguke ndani yake,[d] **34** mwenye shimo hilo anapaswa kulipa.[e] Bei hiyo atamlipa mwenye mnyama, naye mnyama aliyekufa atakuwa wake. **35** Na ikiwa ng'ombe-dume wa mtu atamuumiza ng'ombe-dume wa mtu mwingine naye afe, basi watamuuza ng'ombe-dume aliye hai na kugawana pesa zilizolipwa kwa ajili yake; naye yule aliyekufa pia watagawana.[f] **36** Au ikiwa ilijulikana kwamba ng'ombe-dume huyo alikuwa na zoea la kupiga kwa pembe lakini mwenye ng'ombe-dume huyo hakumzuia,[g] basi lazima atalipa[h] ng'ombe-dume kwa ng'ombe-dume, naye aliyekufa atakuwa wake.

22 "Na mtu akiiba ng'ombe-dume au kondoo na kumchinja au kumuuza, atalipa watano kutoka katika mifugo kwa ajili ya ng'ombe-dume huyo na wanne kutoka katika kundi kwa ajili ya kondoo huyo.[i]

SURA 21
a Met 10:13
b Mwa 9:5; Law 24:17
c Zb 139:16; Yer 1:5
d Kut 18:26; Kum 16:18; Kum 17:8; Kum 22:18; 2Nya 19:10
e Mwa 9:6; Law 24:17; Hes 35:31; Ufu 21:8
f Law 24:20; Amu 1:7; Mt 5:38
g 1Sa 15:33; Mt 7:2
h Efe 6:9; Kol 4:1
i Mwa 9:5; Hes 35:33

Safu ya 2
a Kum 17:8
b Kum 1:17
c Zek 11:12; Mt 27:9
d Mt 12:11; 1Ko 10:24
e Kut 22:6; Kut 22:14; Kum 22:8
f Law 25:17; Mt 7:12
g Met 22:3
h Law 24:21

SURA 22
i 2Sa 12:6; Lu 19:8

2 ("Mwizi[a] akipatikana akifanya tendo la kuvunja[b] ili kuingia naye apigwe na kuuawa, hakuna hatia ya damu kwa ajili yake.[c] **3** Ikiwa jua limeangaza juu yake, basi kuna hatia ya damu kwa ajili yake.)

"Lazima alipe. Ikiwa hana chochote, basi atauzwa kwa ajili ya vitu alivyoiba.[d] **4** Vitu vilivyoibwa vikipatikana pasipo shaka mikononi mwake, ng'ombe-dume, punda, na kondoo, wakiwa hai, atalipa mara mbili.

5 "Mtu akilisha katika shamba au shamba la mizabibu naye aache wanyama wake wa kubeba mizigo wakale katika shamba lingine, atalipa[e] kwa yaliyo bora ya shamba lake mwenyewe au kwa yaliyo bora ya shamba lake mwenyewe la mizabibu.

6 "Moto ukienea na kushika miiba, nayo miganda au nafaka inayosimama au shamba liteketee,[f] yule aliyeuanzisha moto huo lazima alipie kilichoteketea.

7 "Mtu akimpa mwenzake pesa au vitu amwekee,[g] nayo viibiwe kutoka katika nyumba ya mtu huyo, mwizi huyo akipatikana, atalipa mara mbili.[h] **8** Mwizi huyo asipopatikana, basi mwenye nyumba hiyo ataletwa karibu na Mungu wa kweli[i] ili kuona ikiwa hakutia mkono wake juu ya vitu vya mwenzake. **9** Kuhusu kesi yoyote ya ukosaji,[j] inayohusu ng'ombe-dume, punda, kondoo, vazi, kitu chochote kilichopotea ambacho huenda akasema hivi juu yake 'Ndicho hiki!' kesi yao wote wawili italetwa mbele za Mungu wa kweli.[k] Yule ambaye Mungu atamtangaza kuwa mwovu atamlipa mwenzake mara mbili.[a]

10 "Mtu akimpa mwenzake punda au ng'ombe-dume au kondoo au mnyama yeyote wa kufugwa ili aweke, naye mnyama huyo afe au alemae au achukuliwe bila mtu yeyote kuona, **11** kiapo[b] kwa jina la Yehova kinapaswa kifanywe kati yao wawili ya kwamba yeye hakutia mkono wake juu ya mali za mwenzake;[c] na mwenyewe lazima akubali, na yule mwingine hatalipa. **12** Lakini ikiwa kwa kweli wataibiwa kutoka kwake, atamlipa mwenyewe.[d] **13** Ikiwa kwa kweli atararuliwa na mnyama-mwitu,[e] atamleta awe ushuhuda.[f] Hatalipia kitu kilichoraruliwa na mnyama-mwitu.

14 "Lakini mtu yeyote akimwomba mwenzake kitu fulani,[g] nacho kilemae au kife kama mwenyewe hayupo pamoja nacho, lazima atalipa.[h] **15** Ikiwa mwenyewe yupo pamoja nacho, hatalipa. Ikiwa ni cha kukodi, lazima hasara itiwe ndani ya kodi yake.

16 "Sasa, mwanamume akimshawishi bikira ambaye hajachumbiwa, na alale naye,[i] lazima atamchukua awe mke wake kwa ile bei ya kununua.[j] **17** Baba yake akikataa kabisa kumpa yeye, mwanamume huyo atalipa pesa hizo kwa kiwango cha bei ya kununua mabikira.[k]

18 "Usimhifadhi hai mwanamke mlozi.[l]

19 "Mtu yeyote anayelala na mnyama lazima atauawa.[m]

20 "Mtu anayetoa dhabihu kwa miungu yoyote isipokuwa kwa Yehova peke yake ataangamizwa.[n]

SURA 22
a Kut 20:15
Ro 13:9
1Ko 6:10
Efe 4:28
1Pe 4:15
b Yer 2:26
Mt 6:20
Mt 24:43
c Hes 35:27
d Mt 18:25
e Ebr 2:2
f 2Sa 14:30
g Mt 25:14
h Kut 22:4
i Kum 16:18
Kum 19:17
Zb 82:1
j Kut 23:21
k Kut 18:22
Kum 16:18
Kum 25:1
1Sa 2:25
2Nya 19:10

Safu ya 2
a Kut 22:4
b Ebr 6:16
c Law 6:3
Met 30:9
d Mwa 31:39
e Eze 4:14
f Mwa 37:33
Amo 3:12
g Zb 37:21
Met 22:7
h Kut 21:34
Law 24:18
i Mwa 34:2
Kum 22:28
j Mwa 34:12
k Kum 22:29
l Law 19:26
Law 20:6
Kum 18:10
1Sa 28:3
Ga 5:20
Ufu 22:15
m Law 18:23
Law 20:15
Kum 27:21
n Hes 25:3
1Fa 18:40
2Fa 10:25
1Ko 10:20

21 "Na usimtendee vibaya
mkaaji mgeni wala kumkandamiza,[a] kwa sababu ninyi mlikuwa wakaaji wageni katika nchi
ya Misri.[b]
22 "Msimtese mjane yeyote
wala mvulana asiye na baba.[c]
23 Mkimtesa hata kidogo,
naye anililie hata kidogo, sitakosa kukisikia kilio chake;[d]
24 nayo hasira yangu itawaka kwelikweli,[e] nami hakika nitawaua kwa upanga, na wake
zenu watakuwa wajane, nao
wana wenu watakuwa wavulana wasio na baba.[f]
25 "Ukiwakopesha watu wangu pesa, mwenye kuteseka aliye kando yako,[g] usiwe kwake kama mla-riba. Msimtoze fa-
ida.[h]
26 "Ukichukua vazi la mwenzako kuwa rehani,[i] yakupasa ulirudishe kwake wakati wa
kutua kwa jua. **27** Kwa maana hilo ndilo vazi pekee la kujifunika alilo nalo.[j] Ndiyo nguo
yake ya kujitanda ili kuifunika ngozi yake. Atalalia nini?
Na itakuwa kwamba atanililia,
nami hakika nitasikia, kwa sababu mimi ni mwenye neema.[k]
28 "Usimlaani Mungu[l] wala
kumlaani mkuu kati ya watu
wako.[m]
29 "Mazao yako kamili na
ziada ya shinikizo lako usitoe
kwa kusitasita.[n] Mzaliwa wa
kwanza wa wana wako uta-
nipa mimi.[o] **30** Hivi ndivyo
utakavyofanya kuhusu ng'o-
mbe-dume wako na kondoo
wako:[p] Siku saba atakaa na
mama yake.[q] Siku ya nane uni-
pe mimi.
31 "Nanyi lazima muwe
watu watakatifu kwangu;[r] na-
nyi msile nyama shambani
ambayo imeraruliwa na mnya-
ma-mwitu.[a] Mtawatupia mbwa
nyama hiyo.[b]

23 "Usieneze habari isiyo ya
kweli.[c] Usishirikiane na
mtu mwovu kwa kuwa shahidi
anayepanga jeuri.[d] **2** Usiufu-
ate umati kwa ajili ya makusu-
dio maovu;[e] wala usishuhudie
juu ya ubishi ili kugeuka kando
pamoja na umati kwa kusudi
la kupotosha haki.[f] **3** Na kwa
ajili ya mtu wa hali ya chini, usi-
onyeshe upendeleo katika ubi-
shi wake.[g]
4 "Ukikutana na ng'ombe-
dume au punda wa adui yako
akipotea, lazima umrudishe
kwake.[h] **5** Ukimwona punda
wa mtu anayekuchukia akiwa
amelala chini ya mzigo wake,
basi lazima ujizuie usimwache.
Lazima utamfungua pamoja
naye.[i]
6 "Usipotoshe uamuzi wa
hukumu wa mtu wako aliye ma-
skini katika ubishi wake.[j]
7 "Utakaa mbali na neno la
uwongo.[k] Nawe usimuue mtu
asiye na hatia na yule aliye
mwadilifu, kwa maana sitamta-
ngaza mwovu kuwa mwadilifu.[l]
8 "Usikubali rushwa, kwa
maana rushwa hupofusha watu
wanaoona vizuri na inaweza
kupotosha maneno ya watu wa-
adilifu.[m]
9 "Nawe usimkandamize
mkaaji mgeni,[n] kwa maana ni-
nyi wenyewe mmeijua nafsi ya
mkaaji mgeni, kwa sababu mli-
kuwa wakaaji wageni katika
nchi ya Misri.[o]
10 "Na kwa miaka sita uta-
panda mbegu katika shamba
lako nawe utakusanya mazao
yake.[p] **11** Lakini mwaka wa

SURA 22
a Law 19:33
Law 25:35
Zek 7:10
b Kum 10:19
Mdo 7:6
c Kum 27:19
Zb 94:6
Isa 1:17
Eze 22:7
Yak 1:27
d Ayu 34:28
Zb 10:18
Lu 18:7
Yak 5:4
e Zb 69:24
Ebr 10:31
f Kum 32:35
Zb 109:9
g Law 25:35
h Law 25:36
Kum 23:19
Ne 5:7
Lu 6:35
i Kum 24:6
Ayu 24:9
Amo 2:8
j Kum 10:18
Kum 24:13
Ayu 24:10
k Zb 34:6
Efe 2:7
l Law 24:14
Yoh 10:36
Yud 15
m Mhu 10:20
Mdo 23:5
2Pe 2:10
Yud 8
n Met 3:9
2Ko 9:7
o Kut 13:2
p Kum 15:19
q Law 22:27
r Law 19:2
Hes 15:40
1Pe 1:15

Safu ya 2
a Law 22:8
Eze 4:14
Mdo 10:14
b 1Fa 14:11
Yer 15:3

SURA 23
c Law 19:16
Met 6:19
Met 10:18
Yoh 8:44
d Kum 19:18
Met 19:5
Mt 26:59
Mdo 6:11
Ufu 12:10
e Met 1:10
Met 1:11
1Ko 15:33
1Pe 4:4
f Ayu 31:34
Lu 23:23
Mdo 25:9
Ro 1:32
g Law 19:15
Yak 3:17
h Met 25:21
1Th 5:15
i Kum 22:4
Lu 6:27
Ro 12:21
j Kum 16:19
2Nya 19:7
Amo 5:12
k Law 19:11
Lu 3:14
Efe 4:25

l Met 17:15; Nah 1:3; Ro 1:18; Ro 2:6; m 1Sa 8:3; 1Sa 12:3; Met 17:23; Mhu 7:7; n Eze 22:7; o Law 19:34; Kum 10:19; p Law 25:3.

saba utaliacha bila kulimwa
nawe utaliacha lipumzike,[a] nao
maskini wa watu wako wata-
kula kutokana nalo; nacho kile
ambacho wataacha kitaliwa na
wanyama wa mwituni.[b] Hivyo
ndivyo utakavyofanya na sha-
mba lako la mizabibu na sha-
mba lako la mizeituni.
12 "Siku sita utafanya kazi
yako;[c] lakini siku ya saba utaa-
cha, ili ng'ombe-dume wako na
punda wako wapate kupumzi-
ka na mwana wa kijakazi wako
na mkaaji mgeni wapate kuji-
burudisha.[d]
13 "Nanyi mtajilinda kuhusi-
ana na yote hayo ambayo nime-
waambia ninyi;[e] nanyi msilitaje
jina la miungu mingine. Lisisi-
kiwe kinywani mwako.[f]
14 "Mara tatu kwa mwa-
ka utanifanyia sherehe.[g]
15 Utaishika sherehe ya keki
zisizo na chachu.[h] Utakula keki
zisizo na chachu[i] siku saba,
kama vile ambavyo nimekua-
muru, wakati uliowekwa katika
mwezi wa Abibu,[j] kwa sababu
katika mwezi huo ulitoka Misri.
Nao wasionekane mbele zangu
mikono mitupu.[k] **16** Pia, she-
rehe ya mavuno ya matunda ya
kwanza yaliyoiva[l] ya kazi zenu,
ya vitu mnavyopanda shamba-
ni;[m] na sherehe ya kukusanya
mwishoni mwa mwaka, wakati
ambapo mnakusanya kazi zenu
kutoka shambani.[n] **17** Pindi
tatu katika mwaka kila mwa-
namume wa kwako ataonekana
mbele za uso wa Bwana wa kwe-
li, Yehova.[o]
18 "Msitoe dhabihu damu ya
dhabihu yangu pamoja na kitu
kilicho na chachu. Nayo ma-
futa ya sherehe yangu yasikae
usiku kucha mpaka asubuhi.[p]
19 "Yaliyo bora zaidi kati ya
matunda ya kwanza yaliyoiva
ya udongo wako utayaleta ka-
tika nyumba ya Yehova Mungu
wako.[a]
"Usimtokose mwana-mbuzi
katika maziwa ya mama yake.[b]
20 "Tazama, ninamtuma ma-
laika[c] mbele yako ili akuongoze
barabarani na kukuingiza ma-
hali ambapo nimetayarisha.[d]
21 Jiangalie kwa sababu yake
na kuitii sauti yake. Usijiende-
she kwa kumwasi yeye, kwa
maana hatawasamehe kosa
lenu;[e] kwa sababu jina langu
limo ndani yake. **22** Hata hi-
vyo, ukiitii sauti yake kabisa
na kwa kweli ufanye yote ni-
takayosema,[f] basi hakika nita-
waonyesha adui zako uadui na
kuwasumbua wale wanaokusu-
mbua.[g] **23** Kwa maana malai-
ka wangu ataenda mbele yako
naye kwa kweli atakuongoza
kwa Waamori na Wahiti na Wa-
perizi na Wakanaani, na Wahivi
na Wayebusi, nami hakika nita-
wafutilia hao mbali.[h] **24** Usii-
namie miungu yao wala kucho-
chewa kuitumikia, wala usifa-
nyize chochote kilicho kama
kazi zao,[i] bali lazima utawaa-
ngusha nawe lazima uzivunje
nguzo zao takatifu.[j] **25** Nanyi
mtamtumikia Yehova Mungu
wenu,[k] naye hakika ataubari-
ki mkate wako na maji
yako;[l] nami kwa kweli nitage-
uzia mbali ugonjwa kutoka ka-
tikati yako.[m] **26** Wala haku-
takuwa na mwanamke ambaye
mimba yake itatoka wala mwa-
namke tasa katika nchi yako.[n]
Nitafanya hesabu ya siku zako
itimie.[o]
27 "Na nitatuma mbele yako
hali ya kuniogopa,[p] nami ha-
kika nitawavuruga watu wote
utakaoingia katikati yao, nami

SURA 23

a Law 25:4
b Zb 147:9
c Kut 20:9
Lu 13:14
d Kum 5:14
e Kum 4:9
1Ti 4:16
Ebr 12:15
f Kum 12:3
Yos 23:7
Ho 2:17
g Kum 16:16
h Law 23:6
Lu 22:7
i 1Ko 5:8
j Kut 12:18
k Kum 16:17
l Yak 1:18
Ufu 14:4
m Law 23:10
Hes 28:26
Kum 16:9
Mdo 2:1
n Kum 16:13
Ne 8:14
Yoh 7:2
Yoh 7:37
o Kum 12:5
p Kut 12:10
Law 7:15

Safu ya 2

a Kut 34:26
Hes 18:12
Ne 10:35
1Ko 15:20
b Kum 14:21
Met 12:10
c Kut 14:19
d Hes 20:16
e Hes 14:35
Yos 24:19
Ebr 12:25
f Kut 19:5
Kum 30:8
g Mwa 12:3
Kum 30:7
h Kut 34:11
Yos 5:13
Yos 24:8
i Kut 20:5
Law 18:3
Kum 12:30
2Nya 33:2
j Kut 20:3
Hes 33:52
2Nya 34:3
k Kum 6:13
Kum 10:12
Yos 22:5
Mt 4:10
l Kum 7:13
Mal 3:10
m Kum 7:15
Zb 103:3
n Kum 7:14
Kum 28:4
o Kut 20:12
Zb 92:14
p Kum 2:25
Yos 2:9

kwa kweli nitakupa shingo za
adui zako wote.[a] **28** Nami ni-
taituma mbele yako hisia ya ku-
vunjika moyo,[b] nayo itawafuku-
zia mbali Wahivi, Wakanaani
na Wahiti kutoka mbele yako.[c]
29 Sitawafukuza kutoka mbe-
le yako kwa mwaka mmoja,
ili nchi isiwe mahame yenye
ukiwa nao wanyama wa mwitu-
ni waongezeke kwelikweli juu
yako.[d] **30** Nitawafukuza ku-
toka mbele yako hatua kwa ha-
tua, mpaka uongezeke na kui-
miliki nchi hiyo kabisa.[e]
31 "Nami nitauweka mpaka
wako kutoka Bahari Nyekundu
hadi bahari ya Wafilisti na ku-
toka nyikani hadi kwenye Mto;[f]
kwa sababu nitawaweka waka-
aji wa nchi hiyo mikononi mwe-
nu, na hakika wewe utawafuku-
zia mbali kutoka mbele yako.[g]
32 Hutafanya agano pamoja
nao au miungu yao.[h] **33** Wa-
sikae katika nchi yako, wasi-
je wakakufanya unitendee dha-
mbi. Ikiwa utaitumikia miungu
yao, itakuwa mtego kwako."[i]

24 Naye akamwambia Musa:
"Panda uende kwa Ye-
hova, wewe na Haruni, Nada-
bu na Abihu[j] na wanaume wa-
zee 70[k] wa Israeli, nanyi mta-
inama mkiwa mbali. **2** Naye
Musa peke yake atamkaribia Ye-
hova; lakini wao wasikaribie,
wala watu wasipande kwenda
pamoja naye."[l]
3 Kisha Musa akaja na ku-
wasimulia watu maneno yote
ya Yehova na maamuzi yote ya
hukumu,[m] nao watu wote wa-
kajibu kwa sauti moja na kusе-
ma: "Maneno yote ambayo Ye-
hova amesema tuko tayari ku-
yafanya."[n] **4** Basi Musa akaa-
ndika maneno yote ya Yehova.[o]
Kisha akaamka asubuhi na ma-

SURA 23
a Kum 7:23
b Kum 7:20
Yos 2:11
c Yos 24:11
d Kum 7:22
e Kum 9:4
Zb 80:8
f Mwa 15:18
Kum 1:7
Yos 1:4
1Fa 4:21
g Amu 1:4
Amu 11:21
h Kut 34:12
Hes 25:2
Kum 7:2
2Ko 6:14
i Yos 23:13
Amu 1:28
Amu 2:3
Zb 106:36

SURA 24
j Law 10:1
1Nya 6:3
k Hes 11:16
l Kut 20:21
Hes 12:8
m Kut 21:1
Kum 4:1
Ebr 8:6
n Kum 5:27
Yos 24:22
o Kut 34:27
Kum 31:9

Safu ya 2
a Yos 4:8
b Law 3:1
Law 7:11
c Ebr 9:18
d Law 17:11
e Kut 34:27
f Kum 31:11
Mdo 13:15
g Kut 19:8
h Ebr 9:19
Ebr 12:24
i Ga 3:19
Ga 3:24
Kol 2:17
Ebr 9:20
Ebr 10:1
j Kut 24:11
Isa 6:1
Yoh 1:18
k Eze 1:26
Ufu 4:3
l Kut 24:1
m Hes 12:6
n Mwa 31:54
Kut 18:12
1Ko 10:18
o Kum 5:22
Mt 5:19

pema na kujenga kwenye se-
hemu ya chini ya huo mlima
madhabahu na nguzo kumi na
mbili zinazolingana na yale ma-
kabila kumi na mawili ya Israe-
li.[a] **5** Baadaye akawatuma vi-
jana kati ya wana wa Israeli
nao wakatoa dhabihu za kute-
keetezwa na kutoa ng'ombe-
dume wakiwa dhabihu, kama
dhabihu za ushirika[b] kwa Yeho-
va. **6** Kisha Musa akachukua
nusu ya damu na kuitia kati-
ka mabakuli,[c] na nusu ya damu
akainyunyiza juu ya madhaba-
hu.[d] **7** Mwishowe akachukua
kitabu cha agano[e] na kukiso-
ma katika masikio ya watu.[f]
Kisha wakasema: "Yote amba-
yo Yehova amesema tuko ta-
yari kuyafanya na kuyatii."[g]
8 Basi Musa akaichukua damu
na kuinyunyiza juu ya watu[h]
na kusema: "Tazama, hii ndiyo
damu ya agano[i] ambalo Yehova
amefanya pamoja nanyi kuhu-
su maneno yote haya."
9 Na Musa na Haruni, Na-
dabu na Abihu na watu 70 kati
ya wanaume wazee wa Israe-
li wakapanda juu, **10** nao wa-
kamwona Mungu wa Israeli.[j]
Na chini ya miguu yake pa-
likuwa na kitu kilichofana-
na na mawe bapa ya yakuti na
kama mbingu kwa kutakata.[k]
11 Naye hakuunyoosha mkono
wake juu ya wale wanaume ma-
shuhuri kati ya wana wa Israe-
li,[l] bali walipata maono ya Mu-
ngu wa kweli,[m] wakala na ku-
nywa.[n]
12 Sasa Yehova akasema na
Musa: "Njoo kwangu juu mli-
mani, ukae huko, kwa maa-
na nataka kukupa mabamba ya
mawe na sheria na amri amba-
yo nitaiandika ili kuwafundi-
sha wao."[o] **13** Basi Musa na

Yoshua mhudumu wake wakasimama, naye Musa akapanda
kwenda juu katika mlima wa
Mungu wa kweli.[a] **14** Lakini
alikuwa amewaambia wale wa-
naume wazee: "Ninyi tungojeeni
mahali hapa mpaka turudi
kwenu.[b] Na, tazama! Haruni na
Huru[c] wako pamoja nanyi. Yeyo-
te aliye na kesi, na awaendee."[d]
15 Basi Musa akaenda juu ka-
tika mlima, huku wingu likiu-
funika mlima huo.[e]

16 Na utukufu[f] wa Yehova
ukaendelea kukaa juu ya Mlima
Sinai,[g] nalo wingu likaendelea
kuufunika kwa siku sita. Mwi-
showe katika siku ya saba aka-
mwita Musa kutoka katikati
ya lile wingu.[h] **17** Na macho-
ni pa wana wa Israeli, kuoneka-
na kwa utukufu wa Yehova ku-
likuwa kama moto[i] wenye kute-
keteza juu ya kilele cha mlima.
18 Kisha Musa akaingia kati-
kati ya wingu na kwenda juu
katika mlima.[j] Naye Musa aka-
kaa mlimani siku 40, mchana
na usiku.[k]

25 Naye Yehova akasema na
Musa,[l] na kumwambia:
2 "Sema na wana wa Israeli,
kwamba wanichukulie mcha-
ngo: Kutoka kwa kila mtu
ambaye moyo wake unamcho-
chea ninyi mtauchukua mcha-
ngo wangu.[m] **3** Na huu ndio
mchango ambao mtauchukua
kutoka kwao: dhahabu[n] na fe-
dha[o] na shaba,[p] **4** na uzi wa
bluu, na sufu iliyotiwa rangi ya
zambarau, na kitambaa chenye
rangi nyekundu ya kochinili,
na kitani bora, na manyoya ya
mbuzi,[q] **5** na ngozi za kondoo-
dume zilizotiwa rangi nyeku-
ndu, na ngozi za sili, na mbao
za mshita;[r] **6** mafuta ya mwa-
nga,[s] mafuta ya zeri[t] kwa aji-
li ya kutia mafuta[a] na kwa aji-
li ya uvumba uliotiwa manuka-
to;[b] **7** na mawe ya shohamu
na mawe ya kuwekwa kwenye
efodi[c] na kwenye kile kifuko
cha kifuani.[d] **8** Nao watani-
fanyia patakatifu, kwa maa-
na mimi nitakaa katikati yao.[e]
9 Kulingana na yote ninayoku-
onyesha wewe kuwa mfano wa
maskani na mfano wa vyombo
vyake vyote, hivyo ndivyo mta-
kavyoifanya.[f]

10 "Nao watafanya Sanduku
la mbao za mshita,[g] mikono mi-
wili na nusu urefu wake na
mkono mmoja na nusu upana
wake na mkono mmoja na nusu
kimo chake. **11** Nawe utalifu-
nika kwa dhahabu safi.[h] Utali-
funika upande wa ndani na wa
nje, nawe utalifanyia ukingo wa
dhahabu kuzunguka juu yake
pande zote.[i] **12** Nawe utate-
ngeneza pete nne za dhahabu
kwa ajili yake na kuziweka juu
ya miguu yake minne, pete mbi-
li upande wake mmoja na pete
mbili upande wake mwingine.[j]
13 Nawe utafanya miti
ya mshita na kuifunika kwa
dhahabu.[k] **14** Nawe utaitia
miti hiyo kwenye zile pete zi-
lizo kwenye pande za Sanduku
ili kuitumia kulibeba Sanduku.
15 Miti hiyo itakaa kwenye
pete za Sanduku. Haitaondole-
wa.[l] **16** Nawe utaweka katika
Sanduku hilo ushuhuda nitaka-
okupa.[m]

17 "Nawe utafanya kifuniko
cha dhahabu safi, mikono miwi-
li na nusu urefu wake na mkono
mmoja na nusu upana wake.[n]
18 Nawe utafanya makerubi
wawili wa dhahabu. Utawafa-
nya kwa kazi ya kufua kwe-
nye miisho miwili ya kifuniko.[o]
19 Na ufanye kerubi mmoja
mwisho huu na kerubi mmo-

SURA 24
a Kut 24:2
Hes 11:28
b Kut 32:1
c Kut 17:10
d Kut 18:26
e Kut 19:9
f Kut 16:10
Law 9:23
Hes 16:42
Eze 1:28
g Kut 19:11
h Mt 17:5
i Kut 3:2
Kum 4:24
Eze 1:27
Ebr 12:29
j Kut 19:20
k Kut 34:28
Kum 9:9
1Fa 19:8
Mt 4:2

SURA 25
l Mdo 7:53
Ga 3:19
m Kut 35:5
1Nya 29:9
2Ko 9:7
n Kut 38:24
o Kut 38:25
p Kut 38:3
Kut 38:29
q Kut 35:6
r Kut 36:20
s Kut 27:20
t Kut 35:8

Safu ya 2
a Kut 30:23
b Kut 30:34
c Kut 28:6
d Kut 28:15
e Kut 29:45
1Fa 6:13
Ebr 9:11
f 1Nya 28:12
Mdo 7:44
Ebr 8:5
Ebr 9:9
g Kut 37:1
h Kut 37:2
Ebr 9:4
i Kut 30:3
j Kut 37:5
k Kut 30:5
1Nya 15:15
l 1Fa 8:8
m Kut 16:34
Kut 31:18
Kut 40:20
Hes 17:10
Kum 31:26
1Fa 8:9
Ebr 9:4
n Kut 37:6
o 1Sa 4:4
Ebr 9:5

ja mwisho ule.[a] Juu ya kifuniko mtawafanya makerubi hao kwenye miisho yake miwili. **20** Na makerubi hao watakuwa wamenyoosha mabawa yao kuelekea juu, wakifunika kifuniko hicho kwa mabawa yao, nyuso zao zikielekeana.[b] Nyuso za makerubi hao zitaelekea kifuniko. **21** Nawe utakiweka kifuniko[c] hicho juu ya Sanduku, na ndani ya Sanduku utaweka ushuhuda nitakaokupa. **22** Nami nitakutokea hapo na kusema nawe toka juu ya kifuniko[d] hicho, toka katikati ya wale makerubi wawili walio juu ya sanduku la ushuhuda, naam, yote nitakayokuamuru wewe kwa ajili ya wana wa Israeli.[e]

23 "Nawe utafanya meza[f] ya mbao za mshita, mikono miwili urefu wake na mkono mmoja upana wake na mkono mmoja na nusu kimo chake. **24** Nawe utaifunika kwa dhahabu safi, nawe utaifanyia ukingo wa dhahabu kuizunguka pande zote.[g] **25** Nawe utaifanyia mzingo wa upana wa kiganja kuizunguka pande zote, nawe utafanya ukingo wa dhahabu kwa ajili ya mzingo wake kuizunguka pande zote.[h] **26** Nawe utaifanyia pete nne za dhahabu na kuziweka pete hizo kwenye pembe nne za miguu yake minne.[i] **27** Hizo pete zitakuwa karibu na mzingo ili kutegemeza miti ya kuibeba meza hiyo.[j] **28** Nawe utafanya miti ya mshita na kuifunika kwa dhahabu, nao wataitumia kuibeba meza hiyo.[k]

29 "Nawe utafanya sahani zake na vikombe vyake na mitungi yake na mabakuli yake watakayotumia katika kumimina matoleo ya kinywaji. Utavifanya kutokana na dhahabu safi.[a] **30** Nawe utauweka mkate wa wonyesho juu ya meza hiyo mbele zangu daima.[b]

31 "Nawe utafanya kinara cha taa cha dhahabu safi. Hicho kinara cha taa kitafanyizwa kwa kazi ya kufua.[c] Msingi wake, matawi yake, vikombe vyake, vifundo vyake na maua yake vitatoka kwake. **32** Na matawi sita yatatoka pande zake, matawi matatu ya kinara cha taa kutoka upande wake mmoja na matawi matatu ya kinara cha taa kutoka ule upande wake mwingine.[d] **33** Vikombe vitatu vyenye umbo la maua ya mlozi vitakuwa kwenye kila moja la matawi yaliyoko upande mmoja, vifundo na maua vikifuatana, na vikombe vitatu vyenye umbo la maua ya mlozi kwenye kila moja la matawi yaliyoko upande ule mwingine, vifundo na maua vikifuatana.[e] Hivyo ndivyo ilivyo kwa matawi sita yanayotoka katika kile kinara cha taa. **34** Na kwenye kinara cha taa kuna vikombe vinne vyenye umbo la maua ya mlozi, vifundo vyake na maua yake vikifuatana.[f] **35** Na kile kifundo kilicho chini ya matawi mawili chatoka kwake na kifundo kilicho chini ya yale matawi mawili mengine chatoka kwake na kifundo kilicho chini ya matawi mengine mawili chatoka kwake, kwa ajili ya yale matawi sita yanayotoka katika kinara.[g] **36** Vifundo vyake na matawi yake vitatoka kwake. Vyote ni kitu kimoja kilichofuliwa, cha dhahabu safi.[h] **37** Nawe utakifanyia taa saba; na taa hizo zitawashwa, nazo zitaangaza juu ya eneo lililo mbele yake.[i] **38** Na mikasi yake

SURA 25

a Mwa 3:24

b 1Fa 8:7
1Nya 28:18

c Kut 40:20
1Nya 28:11
Ebr 9:5

d Kut 30:6
Law 16:2
Hes 7:89
Amu 20:27
Zb 80:1

e 2Sa 6:2
2Fa 19:15
Isa 37:16

f Kut 40:22
Law 24:6
Hes 3:31
Ebr 9:2

g Kut 37:11

h Kut 37:12

i Kut 37:13

j Kut 37:14

k Kut 37:15

Safu ya 2

a Kut 37:16
Hes 4:7
1Fa 7:50

b Law 24:5
1Sa 21:6
1Nya 9:32
2Nya 13:11
Mt 12:4

c Kut 37:17
Kut 40:24
1Fa 7:49
Ebr 9:2

d Kut 37:18

e Kut 37:19

f Kut 37:20

g Kut 37:21

h Hes 8:4

i Kut 30:8
Law 24:3
Hes 8:2
2Nya 13:11

ya tambi na vyetezo vyake ni
vya dhahabu safi.[a] **39** Atakifanya hicho pamoja na vyombo vyake vyote kwa talanta
ya dhahabu safi. **40** Na uhakikishe kwamba umezifanya kulingana na mfano ulioonyeshwa
mlimani.[b]

26 "Nayo maskani mtaifanya kwa vitambaa kumi
vya mahema,[c] kwa vitambaa
vya kitani bora kilichosokotwa
na uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili.[d] Kwa makerubi,[e] kazi ya mtarizi, utavifanya.
2 Urefu wa kila kitambaa cha
hema utakuwa mikono 28 na
upana wa kila kitambaa utakuwa mikono 4. Vitambaa hivyo
vyote vitakuwa na kipimo kimoja.[f] **3** Vitambaa vitano vitafanyiza mfuatano, kimoja
kikiwa kimeunganishwa na kingine, na vitambaa vitano vitafanyiza mfuatano, kimoja kikiwa kimeunganishwa na kingine.[g] **4** Nawe utafanya vitanzi vya uzi wa bluu kwenye
upindo wa kile kitambaa kimoja kilicho mwisho wa mfuatano; nawe utafanya vivyo hivyo
kwenye upindo wa kitambaa
cha nje kabisa kilicho mahali
pale pengine pa kuungania.[h]
5 Utafanya vitanzi 50 kwenye
kitambaa kimoja, na vitanzi 50
utavifanya kwenye mwisho wa
kitambaa kilicho mahali pale
pengine pa kuungania, vitanzi
vikikabiliana.[i] **6** Nawe utafanya kulabu 50 za dhahabu na
kuviunganisha vitambaa hivyo, kimoja kwa kingine, kwa
kulabu hizo, navyo vitakuwa
maskani moja.[j]

7 "Nawe utafanya nguo za
manyoya ya mbuzi[k] kwa ajili
ya hema juu ya maskani. Utafanya vitambaa kumi na moja
vya mahema. **8** Urefu wa kila
kitambaa utakuwa mikono[a] 30,
na upana wa kila kitambaa utakuwa mikono 4. Vitambaa vyote 11 vitakuwa na kipimo kimoja. **9** Nawe utaviunganisha
vitambaa vitano pamoja, na vitambaa sita pamoja,[b] nawe utakikunja mara mbili kile kitambaa cha sita kilicho upande
wa mbele wa hema. **10** Nawe
utafanya vitanzi 50 kwenye
upindo wa kile kitambaa kimoja, cha nje kabisa kwenye ule
mfuatano, na vitanzi 50 kwenye upindo wa kitambaa kilicho mahali pale pengine pa kuungania. **11** Nawe utafanya
kulabu 50 za shaba[c] na kuzitia
kulabu hizo kwenye vile vitanzi
na kuliunganisha lile hema pamoja, nalo litakuwa kitu kimoja.[d] **12** Nacho kitambaa kitakachobaki kitakuwa cha kuning'inia. Nusu ya kitambaa cha
hema kitakachobaki kitaning'inia upande wa nyuma wa maskani. **13** Na mkono mmoja
wa upande huu na mkono mmoja wa upande ule wa kile kinachobakia katika urefu wa vitambaa utakuwa wa kuning'inia
pande za maskani, ili kuifunika upande huu na upande ule.

14 "Nawe utafanya kifuniko
cha hilo hema, kifuniko cha
ngozi za kondoo-dume zilizotiwa rangi nyekundu na kifuniko
cha ngozi za sili upande wa juu.

15 "Nawe utafanya viunzi[e]
vya mbao za mshita kwa ajili
ya maskani hiyo, vinavyosimama mwishoni. **16** Urefu wa
kiunzi utakuwa mikono kumi,
nao upana wa kila kiunzi utakuwa mkono mmoja na nusu.
17 Kila kiunzi kitakuwa na
ndimi mbili zilizounganishwa

SURA 25
a Kut 37:23
Hes 4:9
b Kut 39:42
Hes 8:4
Mdo 7:44
Ebr 8:5

SURA 26
c Ebr 8:5
Ebr 9:11
d Kut 36:8
e Mwa 3:24
Zb 99:1
f Hes 4:25
1Nya 17:1
g Kut 36:10
h Kut 36:11
i Kut 36:12
j Kut 36:13
Kut 39:33
Ebr 9:9
k Kut 35:26

Safu ya 2
a Kum 3:11
b Kut 36:16
c Kum 8:9
Ayu 28:2
d Kut 36:13
e Hes 4:31

pamoja. Hivyo ndivyo utaka-
vyofanya na viunzi vyote vya
maskani. **18** Nawe utavifa-
nya viunzi vya mbao kwa ajili
ya maskani, viunzi 20 kwa aji-
li ya upande unaokabili Negebu,
upande wa kusini.
19 "Nawe utafanya vikalio[a]
40 vya fedha chini ya vile vi-
unzi 20; vikalio viwili chini ya
kiunzi kimoja pamoja na ndimi
zake mbili, na vikalio viwili chi-
ni ya kile kiunzi kingine pamo-
ja na ndimi zake mbili. **20** Na
kwa ajili ya upande ule mwingi-
ne wa maskani, upande wa ka-
skazini, viunzi 20,[b] **21** na vi-
kalio vyake 40 vya fedha, vika-
lio viwili chini ya kiunzi kimo-
ja na vikalio vingine viwili chini
ya kile kiunzi kingine.[c] **22** Na
kwa ajili ya sehemu za nyu-
ma za maskani kuelekea upa-
nde wa magharibi utafanya vi-
unzi sita.[d] **23** Nawe utafanya
viunzi viwili viwe miimo ya pe-
mbeni ya maskani[e] katika se-
hemu zake mbili za nyuma.
24 Navyo vitakuwa pacha se-
hemu ya chini, navyo vitakuwa
pacha mpaka juu ya kila moja
kwenye pete ya kwanza. Hivyo
ndivyo itakavyokuwa kwa ajili
ya vyote viwili. Vitakuwa miimo miwili ya pembeni. **25** Na
kutakuwa na viunzi vinane na
vikalio vyake vya fedha, vika-
lio kumi na sita, vikalio viwili
chini ya kiunzi kimoja na vika-
lio viwili chini ya kile kiunzi ki-
ngine.
26 "Nawe utafanya miti ya
mshita,[f] mitano kwa ajili ya viu-
nzi vya mbao vya upande mmo-
ja wa maskani, **27** na miti mi-
tano kwa ajili ya viunzi vya
upande ule mwingine wa ma-
skani na miti mitano kwa aji-
li ya viunzi vya upande wa ma-
skani kwa ajili ya zile pande
mbili za nyuma kuelekea upa-
nde wa magharibi.[a] **28** Nao
mti wa katikati ulio katikati ya
viunzi utatoka mwisho mmoja
mpaka mwingine.
29 "Nawe utavifunika vile
viunzi vya mbao kwa dhaha-
bu,[b] na pete zake utazifanya
kwa dhahabu ili zitegemeze ile
miti; nawe utaifunika miti hiyo
kwa dhahabu. **30** Nawe utai-
simamisha maskani kulingana
na ramani yake ambayo umeo-
nyeshwa mlimani.[c]
31 "Nawe utafanya pazia[d] la
uzi wa bluu na sufu iliyoti-
wa rangi ya zambarau na kita-
mbaa chenye rangi nyekundu
ya kochinili na kitani bora kili-
chosokotwa. Atalifanya likiwa
na makerubi,[e] kazi ya mtarizi.
32 Nawe utaliweka juu ya ngu-
zo nne za mshita zilizofunikwa
kwa dhahabu. Misumari yake
itakuwa ya dhahabu. Zinakaa
juu ya vikalio vinne vya fe-
dha. **33** Nawe utaliweka pa-
zia chini ya kulabu na kulileta
sanduku la ushuhuda[f] ndani ya
hilo pazia; nalo pazia litawate-
nganishia Patakatifu[g] na Pata-
katifu Zaidi.[h] **34** Nawe utaki-
weka kifuniko juu ya sanduku
la ushuhuda katika Patakatifu
Zaidi.
35 "Nawe utaiweka meza nje
ya pazia, na kinara cha taa[i]
kitakuwa upande tofauti na
hiyo meza, kitakuwa upande
wa maskani kuelekea kusini;
nayo meza utaiweka upande wa
kaskazini. **36** Nawe utafanya
kisitiri[j] kwa ajili ya mlango wa
hema, kisitiri cha uzi wa bluu
na sufu iliyotiwa rangi ya za-
mbarau na kitambaa chenye
rangi nyekundu ya kochinili
na kitani safi kilichosokotwa,
kazi ya mfumaji. **37** Nawe

SURA 26
a Hes 3:36
b Kut 36:25
c Kut 36:26
d Kut 36:20
Kut 36:27
e Kut 36:28
f Kut 36:31

Safu ya 2
a Kut 36:32
b Kut 12:35
Kut 36:34
c Kut 19:3
Kut 25:9
Kut 27:8
Mdo 7:44
Ebr 8:5
d Kut 36:35
Kut 40:21
Law 16:2
Lu 23:45
Ebr 6:19
Ebr 9:3
Ebr 10:20
e Mwa 3:24
f 1Fa 8:6
Ebr 9:4
g Kut 40:22
Kut 40:26
Ebr 9:2
h Kut 40:21
Law 16:2
1Fa 8:6
Ebr 9:3
Ebr 9:12
Ebr 9:24
i Law 24:3
1Fa 7:49
j Kut 36:37

utakifanyizia kile kisitiri nguzo
tano za mshita na kuzifunika
kwa dhahabu. Vibanio vyake
vitakuwa vya dhahabu. Nawe
utavitengenezea vikalio vitano
vya shaba.

27 "Nawe utafanya madha-
bahu ya mbao za mshi-
ta, mikono mitano urefu wake
na mikono mitano upana wake.
Madhabahu[a] hiyo itakuwa mra-
ba, na kimo chake kitakuwa
mikono mitatu. **2** Nawe uta-
fanya pembe[b] zake kwenye
ncha zake nne. Pembe zake zi-
tatoka kwake, nawe utaifu-
nika kwa shaba.[c] **3** Nawe
utafanya makopo yake ya kuo-
ndolea majivu yake yenye ma-
futa, na sepetu zake, na ma-
bakuli yake, na nyuma zake,
na vyetezo vyake; nawe utavi-
fanya vyombo vyake vyote kwa
shaba.[d] **4** Nawe utaifanyia ki-
unzi cha fito, mtandao wa fito[e]
za shaba; nawe utafanya pete
nne za shaba juu ya mtandao
huo kwenye miisho yake mi-
nne. **5** Nawe utauweka chini
ya ukingo wa madhabahu, chini
upande wa ndani, nao mtandao
huo utakuwa kuelekea katikati
ya madhabahu.[f] **6** Nawe uta-
fanya miti kwa ajili ya madha-
bahu, miti yake ikiwa ya mshi-
ta, nawe utaifunika kwa sha-
ba.[g] **7** Nayo miti yake itai-
ngizwa kwenye zile pete, nayo
miti itakuwa kwenye zile pa-
nde mbili za madhabahu wakati
wa kuibeba.[h] **8** Utaifanya iwe
sanduku la mbao lenye uwa-
zi. Kama vile alivyokuonyesha
mlimani, ndivyo watakavyoi-
fanya.[i]

9 "Nawe utafanya ua[j] wa ma-
skani. Upande kuelekea Nege-
bu, kuelekea kusini, ua utaku-
wa na mapazia ya kitani bora
kilichosokotwa,[a] urefu wa upa-
nde mmoja ukiwa mikono mia
moja. **10** Nazo nguzo zake 20
na vikalio vyake 20 vitakuwa
vya shaba. Misumari ya ngu-
zo na viungo vyake vitaku-
wa vya fedha.[b] **11** Ndivyo pia
utakavyokuwa upande wa ka-
skazini kwa urefu, mapazia
yakiwa mikono 100 kwa ure-
fu, nazo nguzo zake 20 na vika-
lio vyake 20 vitakuwa vya sha-
ba, misumari ya nguzo na viu-
ngo vyake vitakuwa vya fedha.[c]
12 Nao upana wa ua, upande
wa magharibi mapazia yataku-
wa mikono 50, nguzo zake zi-
kiwa 10 na vikalio vyake viki-
wa 10.[d] **13** Nao upana wa ua
upande wa mashariki kuele-
kea macheo ya jua utakuwa mi-
kono 50.[e] **14** Na kutakuwako
na mikono kumi na mitano ya
mapazia upande mmoja, nguzo
zake zitakuwa tatu navyo vi-
kalio vyake vitakuwa vitatu.[f]
15 Nao upande ule mwingine
kutakuwako mikono kumi na
mitano ya mapazia, nguzo zake
zitakuwa tatu na vikalio vyake
vitakuwa vitatu.[g]

16 "Na kwa ajili ya lango la
ua kutakuwa na kisitiri chenye
urefu wa mikono 20, cha uzi
wa bluu na sufu iliyotiwa ra-
ngi ya zambarau na kitambaa
chenye rangi nyekundu ya ko-
chinili na kitani bora kilichoso-
kotwa, kazi ya mfumaji,[h] ngu-
zo zake zikiwa 4 na vikalio vya-
ke 4.[i] **17** Nguzo zote za ua ku-
zunguka pande zote zitakazwa
kwa vifaa vya fedha, navyo vi-
banio vyake vitakuwa vya fe-
dha lakini vikalio vyake vitaku-
wa vya shaba.[j] **18** Urefu wa
ua utakuwa mikono 100,[k] nao
upana utakuwa mikono 50, na-
cho kimo kitakuwa mikono 5,
ya kitani bora kilichosokotwa,

SURA 27
a Kut 38:1
Kut 40:29
2Nya 4:1
Ebr 13:10
b Law 4:25
1Fa 2:28
Zb 118:27
c Kut 38:2
Hes 16:38
1Fa 8:64
d Kut 38:3
Law 16:12
1Fa 7:45
e Kut 35:16
f Kut 38:4
g Kut 38:6
Hes 4:14
h Kut 38:7
Hes 4:15
i Kut 25:40
1Nya 28:12
Mdo 7:44
Ebr 8:5
j Kut 40:8
1Fa 6:36
1Fa 8:64
Zb 84:10
Zb 92:13
Zb 100:4

Safu ya 2
a Kut 38:9
b Kut 38:10
c Kut 38:11
d Kut 38:12
e Kut 38:13
f Kut 38:14
Kut 39:40
g Kut 38:15
h Kut 35:25
Kut 38:18
i Kut 38:19
j Kut 38:17
k Kut 27:9

navyo vikalio vyake vitakuwa
vya shaba. **19** Navyo vyombo
vyote vya hiyo maskani katika
utumishi wake wote, na misu-
mari yake yote ya mahema, na
misumari yote ya ua itakuwa ya
shaba.[a]

20 "Nawe utawaamuru wana
wa Israeli wakupe mafuta safi
ya zeituni zilizopondwa kwa aji-
li ya mwanga, ili kuziwasha
taa daima.[b] **21** Katika hema
la mkutano, nje ya pazia[c] li-
lilo kando ya ule Ushuhuda,
Haruni na wanawe watauwe-
ka kwa utaratibu tangu asubu-
hi mpaka jioni mbele za Yeho-
va.[d] Itakuwa sheria mpaka wa-
kati usio na kipimo kwa vi-
zazi vyao,[e] itakayotekelezwa na
wana wa Israeli.[f]

28 "Na wewe, mlete kari-
bu nawe Haruni ndugu
yako na wanawe pamoja naye
kutoka katikati ya wana wa
Israeli ili awe kuhani kwangu,[g]
Haruni,[h] Nadabu na Abihu,[i]
Eleazari na Ithamari,[j] wana
wa Haruni. **2** Nawe utafanya
mavazi matakatifu kwa ajili ya
Haruni ndugu yako, kwa utu-
kufu na uzuri.[k] **3** Na wewe
mwenyewe utasema na wote
wenye hekima walio na moyo
ambao nimeujaza roho ya he-
kima,[l] nao watayafanya mavazi
ya Haruni ili kumtakasa, ili awe
kuhani kwangu.[m]

4 "Na haya ndiyo mavazi wa-
takayoyafanya: kifuko cha ki-
fuani,[n] na efodi[o] na koti lisi-
lo na mikono[p] na kanzu ye-
nye mirabamiraba, kilemba[q]
na ukumbuu;[r] nao watafanya
mavazi matakatifu kwa ajili
ya Haruni ndugu yako na wa-
nawe, ili awe kuhani kwangu.
5 Na wao wenyewe wataichu-
kua dhahabu na ule uzi wa bluu
na ile sufu iliyotiwa rangi ya za-
mbarau na kile kitambaa cha
rangi nyekundu ya kochinili na
kile kitani bora.

6 "Nao watafanya efodi ya
dhahabu, uzi wa bluu na sufu
iliyotiwa rangi ya zambarau,
kitambaa cha rangi nyekundu
ya kochinili na kitani bora ki-
lichosokotwa, kazi ya mtari-
zi.[a] **7** Nayo itakuwa na vipa-
nde viwili vya begani vitaka-
vyounganishwa kwenye miisho
yake miwili, nayo itaungani-
shwa.[b] **8** Nao mshipi,[c] ulio juu
yake ili kufunga kwa kuikaza,
kulingana na ufundi wake, uta-
kuwa wa vifaa vyake, wa dha-
habu, uzi wa bluu na sufu iliyo-
tiwa rangi ya zambarau na kita-
mbaa chenye rangi nyekundu
ya kochinili na kitani bora kili-
chosokotwa.

9 "Nawe utachukua mawe
mawili ya shohamu[d] na kucho-
nga[e] majina ya wana wa Israeli
juu yake,[f] **10** majina sita juu
ya jiwe moja na yale majina me-
ngine sita yanayobaki juu ya
lile jiwe lingine kulingana na
utaratibu wa kuzaliwa kwao.[g]
11 Kwa kazi ya fundi wa mawe,
kwa mchongo wa muhuri, uta-
yachonga kwenye yale mawe
mawili majina ya wana wa Isra-
eli.[h] Yakiwa yametiwa katika
mapambo ya dhahabu ndivyo
utakavyoyafanya.[i] **12** Nawe
utayaweka yale mawe mawili
juu ya vile vipande vya bega-
ni vya efodi yawe mawe ya uku-
mbusho kwa ajili ya wana wa
Israeli;[j] naye Haruni atayachu-
kua majina yao mbele za Yeho-
va kwenye vipande vyake vi-
wili vya begani ili kuwa uku-
mbusho. **13** Nawe utafanya
mapambo ya dhahabu, **14** na
minyororo miwili ya dhahabu
safi.[k] Utaifanya kama nyuzi,

SURA 27
a Kut 38:20; Hes 3:36
b Kut 39:37; Law 24:2
c Kut 26:33; Kut 40:3; Ebr 6:19; Ebr 9:2; Ebr 9:3; Ebr 10:20
d Kut 30:8; Law 24:3; 2Nya 13:11
e Kut 28:43; Kut 40:15
f Law 21:21; Hes 16:40; Hes 18:23; 2Nya 26:18

SURA 28
g Law 8:2; Ebr 5:1
h Kut 4:14; Zb 99:6; Ebr 5:4
i Kut 6:23; Law 10:1; Hes 26:61
j Kut 38:21; Law 10:16; 1Nya 6:3; 1Nya 24:2
k Kut 29:5; Law 8:7
l Efe 1:17
m Kut 31:6; Kut 36:1; Met 2:6
n Kut 39:8; Kut 39:15; Law 8:8
o Kut 39:2
p Kut 39:22
q Kut 39:28; Kut 39:30; Law 8:9
r Kut 39:29; Law 8:7; Isa 11:5

Safu ya 2
a Kut 39:3
b Kut 39:4
c Kut 29:5
d Mwa 2:12; Kut 35:9
e Kut 39:6; 2Nya 2:7
f Kut 39:14
g Mwa 43:33; Kut 1:1
h Kut 35:27
i Kut 39:13
j Kut 39:7
k Kut 39:15

kwa ufundi wa kamba; nawe
utaiunganisha ile minyororo iliyo kama kamba kwenye yale
mapambo.[a]
15 "Nawe utakifanya kifuko
cha kifuani cha hukumu[b] kwa
ufundi wa mtarizi. Sawa
na ufundi wa efodi utakifa-
nya. Utakifanya kwa dhahabu,
uzi wa bluu na sufu iliyoti-
wa rangi ya zambarau na kita-
mbaa chenye rangi nyekundu
ya kochinili na kitani bora ki-
lichosokotwa.[c] **16** Kinapa-
swa kuwa mraba kinapoku-
njwa, urefu wake ukiwa shubi-
ri moja na upana wake ukiwa
shubiri moja.[d] **17** Nawe utaki-
jaza kwa mawe, kukiwa na mi-
stari minne ya mawe.[e] Mstari
wa zabarijadi,[f] topazi[g] na zu-
maridi[h] ndio mstari wa kwa-
nza. **18** Nao mstari wa pili
utakuwa feruzi,[i] yakuti[j] na ya-
spi.[k] **19** Nao mstari wa tatu
utakuwa jiwe la *leshemi,* akiki[l]
na amethisti.[m] **20** Nao mstari
wa nne utakuwa krisolito,[n] sho-
hamu[o] na yashefi. Matundu ya
dhahabu yanapaswa kuwa kati-
ka vijazio vyake.[p] **21** Na hayo
mawe yatakuwa kulingana na
majina ya wana wa Israeli, wale
kumi na wawili kulingana na
majina yao.[q] Kwa michongo ya
muhuri yatakuwa, kila moja
kulingana na jina lake, kwa aji-
li ya yale makabila kumi na ma-
wili.[r]
22 "Nawe utafanya juu ya
kile kifuko cha kifuani minyo-
ororo yenye shada, iliyosokotwa
kama kamba, ya dhahabu safi.[s]
23 Nawe utafanya pete mbili za
dhahabu juu ya kile kifuko cha
kifuani,[t] nawe utaziweka hizo
pete mbili kwenye miisho mi-
wili ya kile kifuko cha kifua-
ni. **24** Nawe utazitia zile ka-
mba mbili za dhahabu kwenye
zile pete mbili zilizo kwenye mi-
isho ya kile kifuko cha kifuani.[a]
25 Nawe utaitia ile miisho mi-
wili ya zile kamba mbili kati-
ka yale mapambo mawili, nawe
utaitia katika vile vipande vya
begani vya efodi, upande wake
wa mbele.[b] **26** Nawe utafanya
pete mbili za dhahabu na kuzi-
weka kwenye ile miisho miwili
ya kile kifuko cha kifuani kwe-
nye upindo wake ulioko upa-
nde unaoielekea efodi, upande
wa ndani.[c] **27** Nawe utafanya
pete mbili za dhahabu na kuzi-
weka juu ya vile vipande viwi-
li vya begani vya efodi upande
wa chini, mbele yake, karibu
na mahali inapounganikia, juu
ya mshipi wa efodi.[d] **28** Nao
watakifunga kifuko cha kifua-
ni kwa pete zake kwenye zile
pete za efodi kwa uzi wa bluu,
ili kiwe juu ya mshipi wa efodi
nacho kifuko cha kifuani kisio-
ndoke juu ya efodi.[e]
29 "Naye Haruni atayachu-
kua majina ya wana wa Israeli
kwenye kile kifuko cha kifuani
cha hukumu juu ya moyo wake
anapoingia Patakatifu ili uwe
ukumbusho mbele za Yehova
daima. **30** Nawe utaweka Uri-
mu[f] na Thumimu ndani ya kile
kifuko cha kifuani cha huku-
mu, nazo zitakuwa juu ya moyo
wa Haruni anapoingia mbele
za Yehova; naye Haruni atachu-
kua hukumu[g] za wana wa Isra-
eli juu ya moyo wake mbele za
Yehova daima.
31 "Nawe utalifanya koti
lote lisilo na mikono la efo-
di kwa uzi wa bluu.[h] **32** Nalo
litakuwa na sehemu iliyo wazi
katikati yake upande wa juu.
Sehemu hiyo iliyo wazi itaku-
wa na ukingo wa kuizungu-
ka pande zote, kazi ya mfuma-
ji. Sehemu hiyo itakuwa

SURA 28
a Kut 39:18
b Kut 28:30
Law 8:8
Hes 27:21
c Kut 39:8
d Kut 39:9
e Kut 39:10
f Eze 27:16
g Ufu 21:20
h Kut 39:10
Ufu 21:19
i Kut 39:11
j Kut 24:10
Eze 1:26
k Ufu 4:3
Ufu 21:11
l Kut 39:12
m Ufu 21:20
n Wim 5:14
o 1Nya 29:2
p Kut 39:13
q 1Fa 18:31
r Kut 1:1
s Kut 39:15
t Kut 39:16

Safu ya 2
a Kut 39:17
Law 8:8
b Kut 39:18
c Kut 39:19
d Kut 28:8
Kut 39:20
Law 8:7
e Kut 39:21
f Law 8:8
Hes 27:21
Kum 33:8
1Sa 28:6
Ezr 2:63
g Isa 58:2
Yoh 8:16
Ebr 4:15
Ebr 5:1
h Kut 39:22
Law 8:7

kama ile sehemu wazi ya vazi
la chuma, ili isipate kurarulivwa.[a] **33** Nawe utafanya kwe-
nye upindo wake makomama-
nga ya uzi wa bluu na sufu iliyo-
tiwa rangi ya zambarau na kita-
mbaa chenye rangi nyekundu
ya kochinili, kwenye upindo
wake kuuzunguka pande zote,
na kengele[b] za dhahabu katika-
ti yake pande zote; **34** kenge-
le ya dhahabu na komamanga,
kengele ya dhahabu na koma-
manga juu ya upindo wa koti li-
silo na mikono kulizunguka pa-
nde zote.[c] **35** Nalo litakuwa
juu ya Haruni ili apate kuhudu-
mu, nayo sauti kutoka kwake
itasikiwa anapoingia ndani ya
patakatifu mbele za Yehova na
anapotoka nje, ili asife.[d]

36 "Nawe utafanya bamba li-
nalong'aa la dhahabu safi na
kulichonga kwa michongo ya
muhuri, 'Utakatifu ni wa Yeho-
va.'[e] **37** Nawe utalikaza kwa
uzi wa bluu, nalo litakuwa juu
ya kilemba.[f] Litakuwa upande
wa mbele wa kilemba.
38 Nalo litakuwa kwenye paji
la uso wa Haruni, naye Haru-
ni atatoa jibu kwa ajili ya kosa
linalofanywa juu ya vyombo vi-
takatifu,[g] ambavyo wana wa
Israeli watatakasa, yaani, zawa-
di zao zote takatifu; nalo lita-
kaa kwenye paji la uso wake
daima, ili kupata kibali kwa aji-
li yao[h] mbele za Yehova.

39 "Nawe utafuma kanzu ya
kitani bora yenye mirabamira-
ba na kufanya kilemba cha ki-
tani bora,[i] nawe utafanya uku-
mbuu,[j] kazi ya mfumaji.

40 "Nao wana wa Haruni
utawafanyia kanzu,[k] nawe uta-
wafanyia ukumbuu kila mmo-
ja wao, nawe utawafanyia ma-
valio ya kichwani[l] kwa utuku-
fu na uzuri.[m] **41** Na kwa vitu

SURA 28
a Kut 39:23
b Kut 39:25
c Kut 39:26
d Law 16:2
Hes 18:7
e Kut 39:30
Law 8:9
1Nya 16:29
Zb 93:5
Zek 14:20
Ebr 7:26
1Pe 1:16
f Kut 29:6
Kut 39:31
g Law 10:17
Law 22:9
Hes 18:1
Isa 53:11
2Ko 5:21
Ebr 9:28
1Pe 2:24
h Law 23:11
Ro 8:34
Ebr 7:25
i Kut 28:4
Ufu 19:8
j Kut 39:29
k Kut 39:27
Law 8:13
1Sa 2:18
l Kut 39:28
Law 8:13
m Kut 28:2

Safu ya 2
a Kut 29:7
Kut 30:30
Law 10:7
Mdo 10:38
2Ko 1:21
1Yo 2:27
b Kut 29:9
Law 8:33
Hes 3:3
c Law 6:10
d Kut 27:21

SURA 29
e Law 8:2
Law 9:2
2Nya 13:9
f Kum 15:21
Kum 17:1
g Law 6:20
Law 7:12
h Law 8:26
i Kut 26:36
Kut 40:28
Law 8:3
j Law 8:6
Ebr 7:26
Ebr 10:22
k Kut 28:4
Law 8:7
Law 16:4
l Kut 28:8

hivyo wewe utamvika Haruni
ndugu yako na wanawe pamo-
ja naye, nawe utawatia mafuta[a]
na kuijaza mikono yao nguvu[b]
na kuwatakasa, nao watakuwa
makuhani kwangu. **42** Na
uwafanyie suruali za kitani ili
kuufunika mwili ulio uchi.[c] Zi-
anzie kiunoni mpaka kwenye
mapaja. **43** Nazo zitavaliwa na
Haruni na wanawe wanapoingia
kwenye hema la mkutano
au wanapoenda karibu na ma-
dhabahu ili kuhudumu katika
mahali patakatifu, ili wasifanye
kosa na kufa hakika. Ni sheria
mpaka wakati usio na kipimo
kwa ajili yake na uzao wake ba-
ada yake.[d]

29 "Na hili ndilo jambo uta-
kalowafanyia ili kuwa-
takasa wapate kuwa makuha-
ni kwangu: Mchukue ng'ombe-
dume mchanga, na kondoo-
dume wawili,[e] wasio na kasoro,[f]
2 na mkate usio na chachu na
keki za mviringo zisizo na cha-
chu, ambazo zimetiwa mafu-
ta na mkate mwembamba usio
na chachu, uliotiwa mafuta.[g]
Utavifanya kutokana na unga
laini wa ngano. **3** Nawe utavi-
tia kwenye kikapu na kuvitoa
vikiwa ndani ya kikapu,[h] hali
kadhalika yule ng'ombe-dume
na wale kondoo-dume wawili.

4 "Nawe utawaweka Haru-
ni na wanawe kwenye mlango[i]
wa hema la mkutano, nawe
utawaosha kwa maji.[j] **5** Ki-
sha utayachukua yale mavazi[k]
na kumvika Haruni kwa ka-
nzu na koti lisilo na mikono
la efodi na kwa efodi na kifu-
ko cha kifuani, nawe utamfu-
nga hicho kwa kukaza kwa
mshipi wa efodi.[l] **6** Nawe uta-
kiweka kilemba juu ya ki-
chwa chake na kuiweka ile

ishara takatifu ya wakfu juu
ya kilemba.[a] **7** Nawe utachu-
kua mafuta yanayotumiwa ku-
tia mafuta na kuyamimina[b]
juu ya kichwa chake na kumtia
mafuta.[c]

8 "Ndipo utakapowaleta wa-
nawe karibu, nawe utawavi-
ka kanzu.[d] **9** Nawe utawafu-
nga ukumbuu, Haruni pamoja
na wanawe, nawe utawafunga
valio la kichwani; nao uku-
hani utakuwa wao, hiyo ikiwa
ni sheria mpaka wakati usio
na kipimo.[e] Basi utajaza nguvu
mkono wa Haruni na mkono
wa wanawe.[f]

10 "Sasa utamtoa yule ng'o-
mbe-dume mbele ya hema la
mkutano, na Haruni na wana-
we wataweka mikono yao juu
ya kichwa cha huyo ng'ombe-
dume.[g] **11** Nawe utamchinja
huyo ng'ombe-dume mbele za
Yehova, kwenye mlango wa
hema la mkutano.[h] **12** Nawe
utachukua sehemu ya damu[i] ya
huyo ng'ombe-dume na kuiwe-
ka kwa kidole chako juu ya zile
pembe za madhabahu,[j] na damu
yote inayobaki utaimimina chi-
ni ya madhabahu.[k] **13** Nawe
utayachukua mafuta yote[l] ya-
nayofunika matumbo,[m] na kile
kipasho kilicho juu ya ini,[n] na
zile figo mbili na mafuta yali-
yo juu yake, nawe utavifukiza
juu ya madhabahu.[o] **14** Laki-
ni nyama ya ng'ombe-dume na
ngozi yake na mavi yake utavi-
teketeza kwa moto nje ya ka-
mbi.[p] Hilo ni toleo la dhambi.

15 "Kisha utamchukua ko-
ndoo-dume mmoja,[q] naye Ha-
runi na wanawe wataweka mi-
kono yao juu ya kichwa cha
kondoo huyo.[r] **16** Nawe uta-
mchinja kondoo huyo na kui-
chukua damu yake na kuinyu-
nyiza kuzunguka pande zote

SURA 29
a Kut 28:36
Kut 39:30
Law 8:9
b Kut 30:25
c Law 8:12
Zb 133:2
Isa 61:1
Mdo 10:38
d Kut 28:40
Law 8:13
e Kut 28:1
Kut 28:43
Kut 40:15
f Kut 28:41
Kut 32:29
Flp 4:13
g Law 8:14
h Law 1:3
Law 1:5
i Law 8:15
j Kut 27:2
k Law 4:7
l Law 3:17
Law 4:8
Zb 69:9
m Law 1:9
Law 9:14
n Law 8:16
Law 9:19
o Law 17:6
p Law 16:27
q Law 8:18
r Law 1:4

Safu ya 2
a Law 8:19
Ebr 9:22
b Law 1:13
Law 8:21
c Mwa 22:2
Law 9:24
d Mwa 8:21
Efe 5:2
Flp 4:18
e Law 8:22
f Law 8:24
g Kut 30:25
Zb 133:2
Isa 61:1
h Law 8:30
i Law 3:9
Law 7:3
Law 9:19
j Law 7:32
Law 9:21
Hes 18:18
k Law 8:22

juu ya madhabahu.[a] **17** Nawe
utamkata kondoo huyo katika
vipande vyake mbalimbali, na
kuyaosha matumbo[b] yake na
miguu yake na kuviweka vi-
pande vyake pamoja hata ki-
chwa chake. **18** Nawe uta-
mfukiza kondoo huyo mzima
juu ya madhabahu. Hilo ni to-
leo la kuteketezwa[c] kwa Yeho-
va, harufu yenye kutuliza.[d] Ni
toleo linalotolewa kwa Yehova
kwa njia ya moto.

19 "Kisha utamchukua yule
kondoo-dume mwingine, naye
Haruni na wanawe wataweka
mikono yao juu ya kichwa cha
kondoo huyo.[e] **20** Nawe uta-
mchinja kondoo huyo na ku-
chukua sehemu ya damu yake
na kuitia kwenye ncha ya si-
kio la kuume la Haruni na kwe-
nye ncha ya sikio la kuume
la wanawe na kwenye kido-
le gumba cha mkono wao wa
kuume na kwenye kidole ki-
kubwa cha mguu wao wa ku-
ume,[f] nawe utainyunyiza damu
hiyo kuzunguka pande zote juu
ya madhabahu. **21** Nawe uta-
chukua sehemu ya damu hiyo
iliyo kwenye madhabahu na se-
hemu ya mafuta yanayotumi-
wa kutia mafuta,[g] nawe utaya-
tapanya juu ya Haruni na ma-
vazi yake na juu ya wanawe na
mavazi ya wanawe walio pamo-
ja naye, ili yeye na mavazi yake
na wanawe na mavazi ya wana-
we walio pamoja naye yapate
kuwa matakatifu kwelikweli.[h]

22 "Nawe utachukua kutoka
kwa kondoo-dume huyo mafu-
ta na ule mkia mnono[i] na yale
mafuta yanayofunika matu-
mbo, na kipasho cha ini, na
zile figo mbili na mafuta yaliyo
juu yake, na mguu wa kuume,[j]
kwa maana huyo ni kondoo wa
kuweka rasmi;[k] **23** Pia mka-

te wa mviringo na keki ya mviringo ya mkate uliotiwa mafuta na mkate mwembamba kutoka katika kile kikapu cha keki zisizo na chachu kilicho mbele za Yehova.[a] **24** Nawe utaviweka vyote hivyo kwenye mikono ya Haruni na kwenye mikono ya wanawe,[b] nawe utavitikisa huku na huku vikiwa toleo la kutikisa mbele za Yehova.[c] **25** Nawe utavichukua kutoka katika mikono yao na kuvifukiza juu ya madhabahu juu ya toleo la kuteketezwa viwe harufu ya kutuliza mbele za Yehova.[d] Ni toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto.[e]

26 "Nawe utachukua kidari cha yule kondoo-dume wa kuweka rasmi,[f] aliye wa Haruni, na kukitikisa huku na huku kikiwa toleo la kutikisa mbele za Yehova, nacho kitakuwa fungu lako. **27** Nawe utakitakasa kidari[g] cha toleo la kutikisa na ule mguu wa fungu takatifu ambao ulitikiswa na ambao ulichangiwa kutoka katika yule kondoo-dume wa kuweka rasmi,[h] kutoka katika kile kilichokuwa cha Haruni na kutoka katika kile kilichokuwa cha wanawe. **28** Nacho kitakuwa cha Haruni na wanawe kulingana na sharti mpaka wakati usio na kipimo, litakalofanywa na wana wa Israeli, kwa sababu hicho ni fungu takatifu;[i] nacho kitakuwa fungu takatifu litakalotolewa na wana wa Israeli. Kutoka katika dhabihu zao za ushirika[j] hilo ndilo fungu lao takatifu kwa Yehova.

29 "Nayo mavazi matakatifu[k] yaliyo ya Haruni yatatumiwa na wanawe[l] baada yake ili kuwatia mafuta[m] wakiwa wameyavaa na kuijaza mikono yao nguvu wakiwa wameyavaa.[a] **30** Kuhani atakayechukua mahali pake kutoka kati ya wanawe na atakayeingia katika hema la mkutano ili kuhudumu katika mahali patakatifu atayavaa kwa siku saba.[b]

31 "Nawe utamchukua yule kondoo-dume wa kuweka rasmi, nawe utaitokosa nyama yake katika mahali patakatifu.[c] **32** Naye Haruni na wanawe wataila[d] nyama ya kondoo huyo na mkate ulio katika kikapu kwenye mlango wa hema la mkutano. **33** Nao watakula vitu ambavyo vimetumiwa kufanya upatanisho ili kuijaza mikono yao nguvu, ili kuwatakasa.[e] Lakini mgeni asivile, kwa maana ni vitakatifu.[f] **34** Na ikiwa nyama yoyote ya dhabihu ya kuweka rasmi na mkate wowote utabaki mpaka asubuhi, basi utateketeza kwa moto kitakachobaki.[g] Kisiliwe, kwa sababu ni kitu kitakatifu.

35 "Nawe utamfanyia Haruni na wanawe hivyo kulingana na yote ambayo nimekuamuru wewe.[h] Utachukua siku saba ili kuijaza mikono yao nguvu.[i] **36** Nawe utamtoa ng'ombe-dume wa toleo la dhambi kila siku kwa ajili ya upatanisho,[j] nawe utaitakasa madhabahu kutokana na dhambi kwa kufanya upatanisho juu yake, nawe utaitia mafuta[k] ili kuitakasa. **37** Utachukua siku saba kufanya upatanisho juu ya madhabahu, nawe utaitakasa[l] ili iwe madhabahu takatifu zaidi.[m] Mtu yeyote atakayegusa madhabahu hiyo atakuwa mtakatifu.[n]

38 "Na hiki ndicho utakachotoa juu ya madhabahu hiyo: wana-kondoo dume kila mmoja akiwa na umri wa mwaka

SURA 29
a Law 8:26
1Ko 5:8
b Law 8:27
c Law 7:30
d Law 8:28
Efe 5:2
e Law 10:13
1Sa 2:28
f Law 8:29
Zb 99:6
g Law 10:15
h Kut 29:22
Law 7:37
i Law 7:34
Law 10:14
Hes 15:19
Hes 18:24
Kum 18:3
j Law 7:11
k Kut 28:4
l Hes 20:26
m Kut 30:30
Kut 40:15
Law 8:12
2Ko 1:21

Safu ya 2
a Kut 28:41
Law 8:33
2Ko 3:5
b Law 8:35
Law 9:1
c Law 8:31
d 1Ko 9:13
1Ko 9:14
e Law 10:13
f Law 22:10
Hes 3:10
Mt 12:4
g Kut 12:10
Law 8:32
h Law 8:4
i Law 8:33
j Law 4:20
k Kut 30:28
Law 8:11
Hes 7:1
l Kut 40:10
m Kut 30:29
Mt 23:19
n Kut 30:29

mmoja, wawili kila siku daima.[a] **39** Nawe utamtoa mwana-kondoo dume mmoja asubuhi,[b] na kumtoa yule mwana-kondoo dume mwingine kati ya zile jioni mbili.[c] **40** Na sehemu ya kumi ya kipimo cha efa ya unga laini[d] uliotiwa sehemu ya nne ya hini ya mafuta yaliyopondwa, na toleo la kinywaji[e] la sehemu ya nne ya hini ya divai, vitatolewa kwa ajili ya yule mwana-kondoo dume wa kwanza. **41** Nawe utamtoa yule mwana-kondoo dume wa pili kati ya zile jioni mbili. Pamoja na toleo la nafaka[f] kama lile la asubuhi na pamoja na toleo la kinywaji kama lake, utamtoa awe harufu ya kutuliza, toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto. **42** Ni toleo la daima[g] la kuteketezwa katika vizazi vyenu vyote kwenye mwingilio wa hema la mkutano mbele za Yehova, ambapo nitajitokeza kwenu ili kusema nanyi hapo.[h]

43 "Nami nitajitokeza hapo kwa wana wa Israeli, napo hakika patatakaswa kwa utukufu wangu.[i] **44** Nami nitalitakasa hema la mkutano na madhabahu; nami nitamtakasa[j] Haruni na wanawe ili wawe makuhani kwangu. **45** Nami nitakaa katikati ya wana wa Israeli, nami nitakuwa Mungu wao.[k] **46** Nao hakika watajua kwamba mimi ni Yehova Mungu wao, aliyewatoa katika nchi ya Misri ili nikae kati yao.[l] Mimi ni Yehova Mungu wao.[m]

30 "Nawe utafanya madhabahu iwe mahali pa kufukizia uvumba;[n] utaifanya kwa mbao za mshita. **2** Urefu wa mkono mmoja na upana wa mkono mmoja, itakuwa mraba, nacho kimo chake kitakuwa mikono miwili. Pembe zake zikiwa zimechomoka kutoka kwake.[a] **3** Nawe utaifunika kwa dhahabu safi, sehemu yake ya juu na sehemu zake za kando kuzunguka pande zote na pembe zake; nawe utaifanyia ukingo wa dhahabu kuzunguka pande zote.[b] **4** Pia utaifanyia pete mbili za dhahabu. Chini ya ukingo wake kwenye pande zake mbili utazifanya, kwenye pande zake mbili zinazoelekeana, kwa kuwa zitakuwa za kutegemeza ile miti ya kuibebea.[c] **5** Nawe utafanya miti ya mshita na kuifunika kwa dhahabu.[d] **6** Nawe utaiweka mbele ya pazia lililo karibu na sanduku la ushuhuda,[e] mbele ya kifuniko kilicho juu ya ule Ushuhuda, mahali ambapo nitajitokeza kwako.[f]

7 "Naye Haruni atafukiza[g] uvumba uliotiwa manukato[h] juu yake. Asubuhi kwa asubuhi, anapotayarisha taa,[i] ataufukiza. **8** Naye Haruni anapowasha taa katikati ya zile jioni mbili, ataufukiza. Ni uvumba wa daima mbele za Yehova katika vizazi vyenu vyote. **9** Hamtatoa juu yake uvumba haramu[j] au toleo la kuteketezwa au toleo la nafaka; wala hamtamimina toleo la kinywaji juu yake. **10** Naye Haruni atafanya upatanisho juu ya pembe zake mara moja kwa mwaka.[k] Kwa sehemu ya damu ya toleo la dhambi[l] la upatanisho ataifanyia upatanisho mara moja kwa mwaka katika vizazi vyenu. Ni takatifu zaidi kwa Yehova."

11 Na Yehova akaendelea kunena na Musa, na kusema: **12** "Wakati wowote unapowahesabu wana wa Israeli,[m] basi

SURA 29
a 1Nya 16:40; 2Nya 2:4; 2Nya 13:11; Da 9:27; Ebr 7:27; Ebr 10:11
b 2Fa 16:15; Mdo 26:7
c Da 9:21
d Kut 16:36; Hes 28:5
e Mwa 35:14; Law 23:13; Flp 2:17
f 1Fa 18:29; Zb 141:2
g Hes 28:6
h Kut 25:22; Law 1:1; Hes 17:4
i Kut 40:34; Hes 12:5; 1Fa 8:11
j Law 21:15; Law 22:9; Yoh 10:36
k Kut 25:8; Law 26:12; Zek 2:11; 2Ko 6:16; Efe 2:22
l Kut 20:2
m Law 11:44; Law 18:30; Law 19:2; Eze 20:5

SURA 30
n Kut 40:5; Zb 141:2

Safu ya 2
a Kut 27:2; Kut 37:25; Law 4:7
b Kut 37:26
c Kut 37:27
d Kut 37:28
e Kut 26:33; Ebr 9:3
f Kut 25:22
g Law 16:13; Hes 16:40; 1Sa 2:28; 1Nya 23:13; Lu 1:9
h Kut 30:34; 2Nya 13:11; Ufu 8:4
i Kut 27:20; 1Sa 3:3
j Law 10:1; 2Nya 26:18; Eze 8:11
k Law 16:18; Law 23:27; Ebr 9:7
l Law 16:5; Law 16:6; Law 16:19
m Kut 38:25; Hes 1:2

kila mmoja wao atamtolea Yehova fidia kwa ajili ya nafsi yake
wakati wa kuhesabiwa kwao,[a]
ili kusiwe na pigo juu yao
wakati wa kuhesabiwa kwao.[b]
13 Hiki ndicho watakachotoa
wale wote wanaopita kwa wale
waliohesabiwa: nusu shekeli ku-
lingana na shekeli ya maha-
li patakatifu.[c] Gera 20 zinato-
shana na shekeli moja. Nusu she-
keli ndio mchango kwa Yehova.[d]
14 Kila mtu anayepita kuingia
upande wa wale walioandiki-
shwa kuanzia umri wa miaka
20 na zaidi atatoa mchango wa
Yehova.[e] **15** Tajiri asitoe zaidi,
naye mtu wa hali ya chini asitoe
kidogo kuliko hiyo nusu sheke-
li,[f] kusudi amtolee Yehova mcha-
ngo ili kufanya upatanisho kwa
ajili ya nafsi zenu.[g] **16** Nawe
utachukua pesa za fedha za upa-
tanisho kutoka kwa wana wa
Israeli na kuzitoa kwa ajili ya
utumishi wa hema la mkutano,[h]
ili kwa kweli uwe ukumbusho
mbele za Yehova na wana wa
Israeli, ili kufanya upatanisho
kwa ajili ya nafsi zenu."

17 Naye Yehova akazidi ku-
sema na Musa, na kumwambia:
18 "Utafanya beseni ya shaba
na kinara chake cha shaba, ya
kuoshea,[i] nawe utaiweka kati
ya hema la mkutano na ile ma-
dhabahu na kutia maji ndani
yake.[j] **19** Naye Haruni na wa-
nawe wataosha mikono yao na
miguu yao kwenye beseni hiyo.[k]
20 Wanapoingia kwenye hema
la mkutano wataoga kwa maji
wasije wakafa, au wanapoenda
karibu na madhabahu kuhudu-
mia ili kumfukizia Yehova toleo
linalotolewa kwa njia ya moto.[l]
21 Nao wataosha mikono yao
na miguu yao wasije wakafa,[m]
nalo litakuwa ni sharti kwao

SURA 30

a Hes 31:50
b 2Sa 24:10
2Sa 24:15
1Nya 21:12
c Law 27:25
d 2Nya 24:9
Ne 10:32
Mt 17:24
e Kut 38:26
Hes 1:3
Hes 26:2
f Ayu 34:19
Met 22:2
Efe 6:9
g Hes 31:50
h Kut 38:25
i Kut 38:8
Law 8:11
1Fa 7:38
j Kut 40:7
k Kut 40:31
Efe 5:26
Ebr 10:22
l 2Nya 13:11
m Kut 40:31

Safu ya 2

a Kut 28:43
2Nya 4:6
b Wim 4:14
Yer 6:20
c Zb 45:8
Wim 1:13
Wim 3:6
d Met 7:17
Ufu 18:13
e Eze 27:19
f Zb 45:8
g Hes 3:47
h Kut 29:40
Law 19:36
Hes 15:5
i Kut 37:29
j Hes 35:25
Zb 89:20
Zb 133:2
Ebr 1:9
k Kut 40:9
Hes 7:1
l Law 8:10
m Kut 29:37
Law 6:18
n Law 8:12
Mdo 10:38
o Hes 3:3
2Ko 1:21
p Kut 40:15
Ufu 5:10
q Kut 37:29
1Fa 1:39
Zb 89:20

mpaka wakati usio na kipimo,
kwake yeye na uzao wake kati-
ka vizazi vyao vyote."[a]

22 Naye Yehova akaendelea
kusema na Musa, na kumwa-
mbia: **23** "Wewe nawe, jichu-
kulie manukato bora zaidi:[b] vi-
pimo 500 vya matone ya mane-
mane[c] iliyoganda, na mdalasini[d]
wenye harufu tamu nusu ya ki-
asi hicho, vipimo 250, na kane[e]
yenye harufu tamu, vipimo 250,
24 na kida,[f] vipimo 500 kuli-
ngana na shekeli ya mahali pa-
takatifu,[g] na mafuta ya zeituni,
hini moja.[h] **25** Kisha utafa-
nya kutokana nayo mafuta ma-
takatifu ya kutia mafuta, ma-
rhamu, mchanganyiko wa kazi
ya mtengenezaji wa marhamu.[i]
Yatakuwa mafuta matakatifu
ya kutia mafuta.[j]

26 "Nawe utayatumia kutia
mafuta lile hema la mkutano[k]
na lile sanduku la ushuhuda,
27 na ile meza na vyombo vya-
ke vyote na kile kinara na vyo-
mbo vyake na ile madhabahu ya
uvumba, **28** na ile madhaba-
hu ya toleo la kuteketezwa na
vyombo vyake vyote na ile be-
seni pamoja na kinara chake.
29 Nawe utavitakasa ili kwa
kweli viwe vitakatifu zaidi.[l]
Yeyote atakayevigusa ataku-
wa mtakatifu.[m] **30** Nawe uta-
mtia mafuta Haruni[n] na wana-
we,[o] nawe utawatakasa wate-
nde wakiwa makuhani kwa-
ngu.[p]

31 "Nawe utanena na wana
wa Israeli, na kusema, 'Haya ya-
taendelea kuwa kwangu mafu-
ta matakatifu ya kutia mafuta,
wakati wa vizazi vyenu vyote.[q]
32 Hayatapakwa kwenye ngo-
zi ya mwanadamu, na kwa
mchanganyiko wake usifanye
mengine yoyote kama hayo.

Ni kitu kitakatifu. Yataendelea
kuwa kitu kitakatifu kwenu.
33 Mtu yeyote anayetengeneza marhamu kama hayo na kumtia mgeni sehemu ya mafuta hayo atakatiliwa mbali kutoka kwa watu wake.'"[a]

34 Naye Yehova akaendelea kumwambia Musa: "Jichukulie manukato:[b] matone ya natafi na shekelethi na kelbena iliyotiwa manukato na ubani[c] safi. Kutakuwa na kipimo kimoja cha kila moja. **35** Nawe utayafanya yawe uvumba,[d] mchanganyo wa viungo, kazi ya mtengenezaji wa marhamu, uliotiwa chumvi,[e] safi, kitu kitakatifu. **36** Nawe utaponda sehemu yake iwe unga laini na kutia kiasi chake fulani mbele ya ule Ushuhuda katika hema la mkutano,[f] nitakapojitokeza kwako.[g] Yatakuwa matakatifu zaidi kwenu. **37** Nao uvumba ambao wewe utaufanya kwa mchanganyiko huo, ninyi hampaswi kuufanya kwa ajili yenu wenyewe.[h] Kwa ajili yenu utaendelea kuwa kitu kitakatifu kwa Yehova.[i] **38** Yeyote atakayefanya wowote ulio kama huo ili kufurahia harufu yake atakatiliwa mbali[j] kutoka kwa watu wake."

31 Naye Yehova akaendelea kusema na Musa, na kumwambia: **2** "Ona, ninamwita kwa jina Bezaleli[k] mwana wa Uri mwana wa Huru wa kabila la Yuda.[l] **3** Nami nitamjaza roho ya Mungu katika hekima na katika uelewaji na katika ujuzi na katika kila aina ya ufundi,[m] **4** kwa ajili ya kubuni vyombo, kwa ajili ya kufanya kazi ya dhahabu na fedha na shaba,[n] **5** na katika kazi ya mawe ili kuyapamba[o] na katika kazi ya mbao ili kufanya kila aina ya vifaa.[a] **6** Mimi nami, tazama! Ninamweka pamoja naye Oholiabu mwana wa Ahisamaki wa kabila la Dani,[b] na katika moyo wa kila mwenye hekima ninaweka hekima, ili kwa kweli wapate kufanya kila kitu ambacho nimekuamuru:[c] **7** lile hema la mkutano[d] na lile Sanduku[e] kwa ajili ya ushuhuda na kifuniko kilicho juu yake,[f] na vyombo vyote vya lile hema, **8** na ile meza na vyombo vyake,[g] na kile kinara cha dhahabu safi na vyombo vyake vyote,[h] na ile madhabahu ya uvumba,[i] **9** na ile madhabahu ya toleo la kuteketezwa na vyombo vyake vyote,[j] na ile beseni na kinara chake,[k] **10** na yale mavazi yaliyofumwa na yale mavazi matakatifu kwa ajili ya Haruni kuhani na yale mavazi ya wanawe kwa ajili ya kutenda wakiwa makuhani;[l] **11** na yale mafuta yanayotumiwa kutia mafuta na ule uvumba uliotiwa manukato kwa ajili ya patakatifu.[m] Kulingana na kila jambo ambalo nimekuamuru, watafanya."

12 Naye Yehova akazidi kusema na Musa: **13** "Wewe nawe, nena na wana wa Israeli, na kusema, 'Hasa sabato zangu, mtazishika,[n] kwa maana ni ishara kati yangu na ninyi katika vizazi vyenu ili mpate kujua kwamba mimi Yehova ninawatakasa ninyi.[o] **14** Nanyi lazima mwishike sabato, kwa maana ni kitu kitakatifu kwenu.[p] Mtu atakayeinajisi hakika atauawa.[q] Ikiwa mtu yeyote atafanya kazi siku hiyo, basi nafsi hiyo itakatiliwa mbali toka katikati ya watu wake.[r] **15** Siku sita kazi inaweza ku-

SURA 30
a Kut 30:38
b Kut 25:6
Kut 37:29
c Law 5:11
Ne 13:5
Wim 3:6
Mt 2:11
d Zb 141:2
Ufu 5:8
e Law 2:13
f Kut 16:34
g Kut 29:42
Law 16:2
h Kut 30:32
i Kut 29:37
j Law 24:16
Hes 15:35

SURA 31
k Kut 37:1
l Kut 35:30
1Nya 2:20
m Kut 35:31
1Fa 7:14
n 2Nya 2:7
o Kut 28:9

Safu ya 2
a Kut 35:33
b Kut 35:34
Kut 38:23
c Kut 36:1
d Kut 36:8
e Kut 37:1
f Kut 37:6
g Kut 37:10
h Kut 35:14
Kut 37:17
i Kut 37:25
j Kut 38:1
Kut 40:6
k Kut 30:18
Kut 38:8
l Kut 28:2
Kut 28:15
Kut 39:1
Kut 39:27
Law 8:7
m Kut 30:25
Kut 30:35
Kut 37:29
n Kut 20:8
Law 19:30
Kol 2:17
o Eze 20:12
Yoh 17:17
1Th 5:23
p Kum 5:12
Isa 56:2
q Eze 20:13
r Kut 35:2
Hes 15:32
Hes 15:35

fanywa, lakini siku ya saba ni
sabato ya pumziko kamili.[a] Ni
kitu kitakatifu kwa Yehova.
Mtu yeyote atakayefanya kazi
siku ya sabato hakika atauawa.
16 Nao wana wa Israeli lazi-
ma waishike sabato, ili kuiti-
miza sabato katika vizazi vyao.
Ni agano mpaka wakati usio
na kipimo.[b] **17** Kati yangu na
wana wa Israeli ni ishara mpa-
ka wakati usio na kipimo,[c] kwa
sababu katika siku sita Yeho-
va alizifanya mbingu na dunia
na katika siku ya saba alipu-
mzika naye akaanza kujiburu-
disha.'"[d]

18 Sasa mara tu alipomaliza
kusema naye kwenye Mlima Si-
nai alimpa Musa mababma ma-
wili ya ule Ushuhuda,[e] maba-
mba ya mawe ambayo juu yake
yaliandikwa kwa kidole cha
Mungu.[f]

32 Wakati huo watu wakao-
na kwamba Musa aliku-
wa akichukua muda mrefu ku-
shuka kutoka mlimani.[g] Basi
watu wakakutanika kumzu-
nguka Haruni na kumwambia:
"Simama, tufanyie mungu ata-
kayeenda mbele yetu,[h] kwa sa-
babu huyo Musa, yule mtu ali-
yetuongoza kutoka katika nchi
ya Misri,[i] hakika hatujui lili-
lompata." **2** Basi Haruni aka-
waambia: "Ng'oeni vipuli vya
dhahabu[j] vilivyo katika masi-
kio ya wake zenu, ya wana wenu
na ya binti zenu mniletee."
3 Nao watu wote wakaanza ku-
ng'oa vipuli vya dhahabu vili-
vyokuwa katika masikio yao na
kuvileta kwa Haruni. **4** Ki-
sha akaichukua dhahabu hiyo
toka mikononi mwao, naye aka-
ifanya[k] kwa kifaa cha kucho-
ngea na kuifanya kuwa sana-
mu ya kuyeyushwa ya ndama.[l]

SURA 31
a Kut 16:23
Kut 20:10
Lu 23:56
b Law 24:8
c Kut 31:13
d Mwa 2:2
Isa 40:28
Ebr 4:4
e Kut 24:12
Kut 32:15
Kum 4:13
Kum 9:15
f Kut 8:19
Mt 12:28
Lu 11:20
2Ko 3:3

SURA 32
g Kut 24:18
Kum 9:9
h Kum 4:15
Yoh 4:24
Mdo 7:40
Mdo 17:29
i Ho 12:13
Mik 6:4
j Kut 12:35
k Kum 9:16
Isa 44:9
Isa 46:6
Mdo 7:41
l 1Fa 12:28
2Fa 10:29
Zb 106:19
Ho 13:2

Safu ya 2
a Kut 20:4
Ne 9:18
Zb 106:20
Ro 1:23
b Mdo 7:41
1Ko 10:7
c Kum 4:16
Kum 9:12
Kum 32:5
Amu 2:19
d Kut 18:20
Kut 20:3
Kum 9:16
Amu 2:17
e 1Fa 12:28
f Kut 34:9
Kum 9:6
Ne 9:16
Mdo 7:51
Ebr 3:15
g Kum 9:14
h Hes 14:12
i Kum 9:18
Zb 106:23
j Kum 9:19
k Hes 14:13

Nao wakaanza kusema: "Huyu
ndiye Mungu wako, Ee Israeli,
aliyekuongoza kutoka nchi ya
Misri."[a]

5 Haruni alipoona hilo, aka-
jenga madhabahu mbele yake.
Mwishowe Haruni akatangaza
na kusema: "Kutakuwa na she-
rehe kwa ajili ya Yehova kesho."
6 Basi siku iliyofuata wakaa-
mka mapema, nao wakaanza
kutoa matoleo ya kuteketezwa
na kutoa dhabihu za ushirika.
Baada ya hayo watu wakaketi
ili wale na kunywa. Kisha wa-
kasimama wapate kujifurahi-
sha.[b]

7 Sasa Yehova akamwambia
Musa: "Nenda, shuka, kwa sa-
babu watu wako ambao uliwa-
ongoza kutoka nchi ya Misri
wametenda kwa uharibifu.[c]
8 Wamegeuka kando hara-
ka kutoka katika njia niliyo-
waamuru waende.[d] Wamejifa-
nyia sanamu ya kuyeyushwa
ya ndama na wanaendelea kui-
namia na kuitolea dhabihu
na kusema, 'Huyu ndiye Mu-
ngu wako, Ee Israeli, aliyekuon-
goza kutoka nchi ya Misri.'"[e]
9 Naye Yehova akaendelea ku-
mwambia Musa: "Nimewataza-
ma watu hawa na, kumbe, ni
watu wenye shingo ngumu.[f]
10 Basi sasa, niache, ili hasi-
ra yangu iwake juu yao nami
niwaangamize,[g] nami nikufa-
nye wewe kuwa taifa kubwa."[h]

11 Naye Musa akaanza ku-
utuliza uso wa Yehova Mungu[i]
wake na kusema: "Kwa nini,
Ee Yehova, hasira[j] yako iwake
juu ya watu wako ambao uli-
watoa katika nchi ya Misri kwa
nguvu kuu na kwa mkono we-
nye nguvu? **12** Kwa nini Wa-
misri[k] waseme, 'Aliwatoa kwa
nia mbaya ili awaue katikati

ya milima na kuwaangamiza
kutoka katika uso wa nchi'?[a] Geukia mbali uiache hasira yako
inayowaka[b] na ujute[c] kuhusu
uovu huo juu ya watu wako.
13 Wakumbuke Abrahamu, Isaka na Israeli watumishi wako,
uliowaapia kwa jina lako mwenyewe,[d] kwa kuwa uliwaambia,
'nitauzidisha uzao wenu kama
nyota za mbinguni,[e] nayo nchi
hii yote ambayo nimeichagua,
nitaupa uzao[f] wenu, ili kwa kweli wapate kuimiliki mpaka wakati usio na kipimo.'"[g]

14 Naye Yehova akaanza kujuta juu ya ule uovu aliokuwa
amesema kwamba atawafanyia
watu wake.[h]

15 Kisha Musa akageuka na
kushuka kutoka mlimani[i] akiwa na yale mabamba mawili
ya Ushuhuda[j] mkononi mwake,
mabamba yaliyoandikwa pande
zote mbili. Yaliandikwa upande huu na upande ule.
16 Nayo mabamba hayo yalikuwa kazi ya Mungu, nayo maandishi yalikuwa maandishi
ya Mungu yaliyochongwa juu
ya mabamba hayo.[k] **17** Naye
Yoshua akaanza kuzisikia kelele za watu kwa sababu ya kupaaza kwao sauti, naye akamwambia Musa: "Kuna kelele
za pigano[l] kambini." **18** Lakini akasema:

"Si sauti ya kuimba kwa
sababu ya tendo lenye
nguvu,[m]
Wala si sauti ya
kuimba kwa sababu ya
kushindwa;
Ni sauti ya uimbaji
mwingine ninayoisikia."

19 Basi ikawa kwamba mara
tu alipoikaribia kambi naye
akaweza kuiona ile ndama[n] na
zile dansi, hasira ya Musa ikaanza kuwaka, naye akayatupa mara moja yale mababa
mawili kutoka mkononi mwake na kuyavunja-vunja chini ya mlima.[a] **20** Kisha
akaichukua ile ndama waliyokuwa wameifanya naye akaiteketeza kwa moto na kuipondaponda mpaka ikawa laini,[b] kisha akaitawanya juu ya
maji[c] na kuwalazimisha wana
wa Israeli wanywe.[d] **21** Kisha Musa akamwambia Haruni:
"Watu hawa walikufanya
nini hivi kwamba umeleta dhambi kubwa juu yao?" **22** Basi
Haruni akasema: "Hasira ya
bwana wangu isiwake. Wewe
mwenyewe unawajua vema watu
hawa, ya kwamba wana mwelekeo mwovu.[e] **23** Basi walini-
ambia, 'Tufanyie mungu atakayeenda mbele yetu,[f] kwa sababu huyo Musa, yule mtu aliyetuongoza kutoka katika nchi
ya Misri, hakika hatujui lililompata.' **24** Basi nikawaambia,
'Ni nani walio na dhahabu yoyote? Waing'oe kutoka kwao
wanipe.' Nami nikaitupa motoni
na ndama hii ikatokea."

25 Naye Musa akaona kwamba watu walikuwa wamejichilia, kwa sababu Haruni alikuwa amewaachilia[g] ili kuwa
fedheha kati ya wapinzani
wao.[h] **26** Kisha Musa akasimama katika lango la kambi
na kusema: "Ni nani aliye upande wa Yehova? Na aje kwangu!"[i] Nao wana wote wa Lawi
wakaanza kujikusanya kwake.
27 Sasa akawaambia: "Hivi
ndivyo Yehova Mungu wa Israeli amesema, 'Kila mmoja wenu
na auweke upanga wake kwenye paja lake. Piteni kati na
kurudi toka lango mpaka la-

SURA 32

a Kum 9:28
b Yos 7:26
c Kum 32:36
2Sa 24:16
d Mwa 22:16
Ebr 6:13
e Mwa 22:17
Mwa 26:4
Mwa 35:11
f Ro 9:7
g Mwa 13:15
h Zb 106:45
Ho 11:9
Yoe 2:13
i Kum 9:15
j Kut 40:20
Kum 5:22
k Kut 31:18
Kut 34:1
Kum 9:10
Kum 10:2
2Ko 3:7
l Yos 6:5
Amo 1:14
m Kut 15:1
n Kum 9:16
Ne 9:18
Zb 106:19
Mdo 7:41

Safu ya 2

a Kum 9:17
b Kum 7:25
Kum 9:21
2Fa 23:6
c Kut 17:6
d Met 1:31
e Kut 15:24
Kut 16:2
Kut 17:2
Kum 9:7
Kum 31:27
f Kut 32:1
Kum 4:15
Mdo 7:40
Mdo 17:29
g 2Nya 28:19
h Kut 32:12
Kum 28:37
i Yos 24:15
2Fa 9:32
2Fa 10:15

ngo katika kambi na kuua kila
mtu ndugu yake na kila mtu
mwenzake na kila mtu rafi-
ki yake.'"[a] **28** Nao wana wa
Lawi[b] wakafanya kama vile
Musa alivyokuwa amesema,
hivi kwamba walianguka kati
ya watu siku hiyo watu wapatao
elfu tatu. **29** Naye Musa aka-
sema: "Ujazeni mkono wenu leo
nguvu kwa ajili ya Yehova,[c] kwa
sababu kila mmoja wenu yuko
dhidi ya mwana wake mwenye-
we na ndugu[d] yake mwenye-
we, na kwamba apate kuweka
baraka juu yenu leo."[e]
30 Na ikawa kwamba siku
ileile iliyofuata, Musa akawaam-
bia watu: "Ninyi—ninyi mme-
tenda dhambi kubwa,[f] na sasa
nitapanda kwenda kwa Yeho-
va. Huenda nitaweza kufanya
upatanisho kwa ajili ya dhambi
yenu."[g] **31** Basi Musa akaru-
di kwa Yehova, akasema: "Ah,
watu hawa wametenda dha-
mbi kubwa, kwa kuwa wame-
jifanyia mungu wa dhahabu![h]
32 Lakini sasa ikiwa utasame-
he dhambi yao,[i]—na ikiwa si-
vyo, nifute,[j] tafadhali, kutoka
katika kitabu[k] chako ambacho
umeandika." **33** Hata hivyo,
Yehova akamwambia Musa:
"Yeyote ambaye amenitendea
dhambi, nitamfutilia mbali ku-
toka katika kitabu changu.[l]
34 Na sasa, njoo, waongoze
watu kwenda mahali nilipokua-
mbia juu yake. Tazama! Malai-
ka wangu ataenda mbele yako,[m]
na siku ile nitakayoleta adhabu
hakika mimi nitaleta adhabu
juu yao kwa sababu ya dhambi
yao."[n] **35** Naye Yehova akaa-
nza kuwaletea watu hao pigo
kwa sababu walikuwa wameifa-
nya ile ndama, ambayo Haruni
alikuwa ameifanya.[o]

SURA 32
a Hes 25:5
Kum 13:8
Zek 13:3
b Kum 33:9
Mal 2:4
c 2Nya 29:31
d Hes 25:11
Kum 13:6
Zek 13:3
e Kum 33:11
f 1Sa 2:17
1Sa 12:20
g Hes 14:20
Hes 16:47
Hes 21:7
Kum 9:18
h Kut 20:23
i Hes 14:19
Isa 1:18
j Kum 9:14
Ro 9:3
k Zb 69:28
Da 12:1
Flp 4:3
Ufu 3:5
Ufu 17:8
l Yer 15:1
Eze 18:4
m Kut 23:20
Kut 33:2
n Amo 3:14
Ro 2:5
o Mdo 7:41

Safu ya 2

SURA 33
a Mdo 7:36
b Mwa 12:7
Mwa 15:6
Mwa 26:3
Ebr 11:9
c Kut 23:20
Kut 32:34
d Kum 7:1
Kum 7:22
Yos 24:11
e Kut 3:8
Kum 8:7
Yos 5:6
Yer 11:5
f Kut 32:9
Kum 9:6
Mdo 7:51
g Kut 32:10
Hes 16:21
h Hes 14:39
Ho 7:14
i Kut 34:9
Zb 78:8
Zb 106:25
j Hes 16:45
Zb 73:19
k Mwa 18:21
Kum 8:2
Zb 139:23
l Kum 9:8
m Kut 18:26
Hes 27:5
n Law 19:32

33 Na Yehova akaendelea
kumwambia Musa: "Ne-
nda, ondoka hapa, wewe
na watu uliowaongoza kuto-
ka nchi ya Misri,[a] mpaka kwe-
nye nchi ambayo nilimwapia
Abrahamu, Isaka na Yakobo, na
kusema, 'Nitaupa uzao wako.'[b]
2 Nami nitamtuma malaika
mbele yako[c] na kuwafukuza
Wakanaani, Waamori, na Wahi-
ti na Waperizi, Wahivi na Wa-
yebusi;[d] **3** kwenye nchi inayo-
tiririka maziwa na asali,[e] kwa
maana sitaenda katikati yenu,
kwa sababu ninyi ni watu we-
nye shingo ngumu,[f] nisije nika-
waangamiza njiani."[g]
4 Watu waliposikia neno hilo
baya, wakaanza kuomboleza;[h]
wala hakuna yeyote kati yao aliy-
evaa mapambo yake. **5** Na
Yehova akaendelea kumwa-
mbia Musa: "Waambie wana wa
Israeli, 'Ninyi ni watu wenye
shingo ngumu.[i] Kwa kitambo
kidogo[j] ningeweza kuingia ka-
tikati yenu na kuwaangami-
za. Sasa vueni mapambo yenu
myaweke chini, kwa maana na-
taka kujua jambo nitakalowate-
ndea ninyi.'"[k] **6** Na wana wa
Israeli wakavua mapambo yao
kuanzia Mlima Horebu[l] na kue-
ndelea.
7 Musa naye akalichukua
hema lake na kulipiga nje ya
kambi, mbali na kambi; naye
akaliita hema la mkutano. Na
ikawa kwamba yeyote aliye-
kuwa akiuliza[m] habari kuto-
ka kwa Yehova alikuwa akie-
nda nje kwenye hema la mku-
tano, lililokuwa nje ya kambi.
8 Na ikatukia kwamba mara
tu Musa alipoenda nje kwenye
hema, watu wote waliinuka,[n]
nao wakasimama kila mmoja
kwenye mlango wa hema lake

mwenyewe, nao wakamtazama
Musa mpaka alipoingia ndani ya
hema. **9** Pia ikatukia kwamba
mara tu Musa alipokuwa ame-
ingia ndani ya hema, ile nguzo
ya wingu[a] ilishuka chini, nayo
ikasimama kwenye mwingilio
wa hema na yeye akasema[b] na
Musa. **10** Na watu wote waka-
iona ile nguzo ya wingu[c] ikisima-
ma kwenye mwingilio wa hema,
nao watu wote wakasimama na
kuinama kila mmoja kwenye
mwingilio wa hema lake mwe-
nyewe.[d] **11** Naye Yehova aka-
sema na Musa uso kwa uso,[e]
kama vile mwanadamu anavyo-
sema na mwenzake. Aliporudi
kambini, mhudumu wake[f] Yo-
shua, mwana wa Nuni,[g] akiwa
mtumishi, hakuwa akiondoka
katikati ya hema.

12 Sasa Musa akamwambia
Yehova: "Angalia, wewe unani-
ambia, 'Waongoze watu hawa,'
lakini hujanijulisha yule amba-
ye utamtuma pamoja nami. Na
zaidi ya hayo, wewe mwenye-
we umesema, 'Ninakujua wewe
kwa jina[h] na, mbali na hayo,
umepata kibali machoni pa-
ngu.' **13** Na sasa, tafadhali,
ikiwa nimepata kibali machoni
pako,[i] nijulishe, tafadhali, njia
zako,[j] nipate kukujua, ili ni-
pate kibali machoni pako. Na
ukumbuke kwamba taifa hili ni
watu wako."[k] **14** Basi akase-
ma: "Mimi mwenyewe nitakwe-
nda pamoja nawe[l] nami hakika
nitakupa wewe pumziko."[m]
15 Ndipo akamwambia: "Iki-
wa wewe mwenyewe hutakwe-
nda pamoja nami, usituongoze
kutoka hapa. **16** Na sasa ita-
julikana jinsi gani kwamba ni-
mepata kibali machoni pako,
mimi na watu wako? Je, si kwa
wewe kwenda pamoja nasi,[n]
kwa kuwa mimi na watu wako
tumefanywa tofauti na watu
wengine wote walio juu ya uso
wa nchi?"[a]

17 Naye Yehova akaendelea
kumwambia Musa: "Jambo hili,
pia, ambalo umesema, nitalifa-
nya,[b] kwa sababu wewe umepata
kibali machoni pangu nami na-
kujua wewe kwa jina." **18** Ndi-
po akasema: "Nionyeshe, tafa-
dhali, utukufu wako."[c] **19** La-
kini akasema: "Mimi mwenyewe
nitaupitisha wema wangu wote
mbele ya uso wako,[d] nami nita-
litangaza jina la Yehova mbele
yako;[e] nami nitamwonyesha ki-
bali yeyote ambaye ninataka
kumwonyesha kibali, nami ni-
tamwonyesha rehema yeyote
ambaye ninataka kumwonye-
sha rehema."[f] **20** Naye akao-
ngezea: "Huwezi kuuona uso wa-
ngu, kwa sababu hakuna mwa-
nadamu anayeweza kuniona na
bado aishi."[g]

21 Naye Yehova akazidi ku-
sema: "Tazama, pana maha-
li kando yangu, nawe utasi-
mama juu ya mwamba. **22** Na
itakuwa kwamba utukufu wa-
ngu utakapokuwa ukipita ni-
takutia katika shimo ndani ya
mwamba, nami nitaweka mko-
no wangu juu yako uwe kisitiri
mpaka niwe nimepita. **23** Ki-
sha nitauondoa mkono wangu,
nawe kwa kweli utauona mgo-
ngo wangu. Lakini uso wangu
hautaonekana."[h]

34 Kisha Yehova akamwa-
mbia Musa: "Jichongee
mabamba mawili ya mawe kama
yale ya kwanza,[i] nami nitaandi-
ka juu ya mabamba hayo mane-
no yaliyokuwa kwenye yale ma-
bamba ya kwanza,[j] ambayo uli-
yavunja-vunja.[k] **2** Nawe ujita-
yarishe kwa ajili ya asubuhi,

SURA 33

a Kut 13:21
Zb 99:7
b Hes 11:17
Hes 12:5
c Kut 40:35
d Kut 4:31
e Mwa 32:30
Kut 33:23
Hes 12:8
Kum 34:10
Yoh 1:18
Yoh 6:46
Mdo 7:38
f Kut 17:9
Kut 24:13
g Hes 11:28
Kum 1:38
Yos 1:1
h Mwa 18:19
Zb 1:6
2Ti 2:19
i Kut 34:9
j Zb 25:4
Zb 27:11
Zb 86:11
Zb 119:33
Isa 30:21
k Kum 9:26
Zb 33:12
l Kut 13:21
Kut 40:34
Yos 1:5
Isa 63:9
m Yos 21:44
Yos 23:1
Yer 6:16
n Hes 14:14

Safu ya 2

a Kum 4:34
2Sa 7:23
Zb 147:20
b Yak 5:16
1Yo 5:14
c Kut 16:10
Kut 24:17
d Lu 2:9
Mdo 7:38
Mdo 7:53
e Kut 3:13
Kut 6:3
Kut 34:6
f Ro 9:15
Ro 9:18
g Kum 5:24
Yoh 4:24
h Kut 33:20
Yoh 1:18

SURA 34

i Kum 10:1
j Kum 9:10
2Ko 3:3
k Kut 32:19
Kum 9:17

kwa kuwa asubuhi utapanda
Mlima Sinai na kusimama ka-
ndo yangu huko juu ya mlima.[a]
3 Lakini mtu yeyote asipande
pamoja nawe, na pia, mtu mwi-
ngine yeyote asionekane kote-
kote katika mlima.[b] Tena, kundi
lolote wala mifugo yoyote isili-
she mbele ya mlima huo."[c]
4 Basi Musa akachonga ma-
bamba mawili ya mawe kama
yale ya kwanza na kuamka asu-
buhi na mapema, akaenda juu
katika Mlima Sinai, kama vile
Yehova alivyokuwa amemwa-
muru, naye alikuwa ameya-
chukua yale mabamba mawi-
li ya mawe mikononi mwake.
5 Naye Yehova akashuka[d] katika
wingu, akasimama huko pa-
moja naye na kulitangaza jina
la Yehova.[e] **6** Na Yehova aka-
pita karibu mbele ya uso wake
na kutangaza: "Yehova, Yeho-
va, Mungu mwenye rehema[f] na
neema,[g] si mwepesi wa hasira[h]
naye ni mwingi wa fadhili zenye
upendo[i] na kweli,[j] **7** anayehi-
fadhi fadhili zenye upendo kwa
ajili ya maelfu,[k] anayesamehe
kosa na ubaya na dhambi,[l] laki-
ni kwa vyovyote hatakosa kua-
dhibu,[m] anayeleta adhabu kwa
ajili ya kosa la akina baba juu
ya wana na juu ya wajukuu, juu
ya kizazi cha tatu na juu ya ki-
zazi cha nne."[n]
8 Mara moja Musa akafanya
haraka kuinama chini na kusu-
judu.[o] **9** Kisha akasema: "Iki-
wa, sasa, nimepata kibali ma-
choni pako, Ee Yehova, tafa-
dhali, Yehova na aende pamoja
nasi katikati yetu,[p] kwa sababu
ni watu wenye shingo ngumu,[q]
nawe utusamehe kosa letu na
dhambi yetu,[r] nawe utuchukue
tuwe mali yako."[s] **10** Naye
akasema: "Tazama, ninafanya

SURA 34

a Kut 19:20
Kut 24:12
b Kut 19:12
c Kut 19:13
Ebr 12:20
d Mdo 7:38
Mdo 7:53
e Kut 6:3
Kut 33:19
f 2Nya 30:9
Ne 9:17
Yoe 2:13
Lu 6:36
Ebr 8:12
g Kut 22:27
Ne 9:31
Zb 86:15
Yon 4:2
h Hes 14:18
Nah 1:3
Ro 9:22
2Pe 3:9
i Yer 31:3
Omb 3:22
Mik 7:18
j Zb 31:5
Ro 2:2
k Yer 32:18
Da 9:4
l Zb 103:12
Isa 55:7
Efe 4:32
1Yo 1:9
m Kum 32:35
Yos 24:19
Ro 2:5
2Pe 2:4
Yud 15
n Kut 20:5
Hes 14:18
Kum 30:19
1Sa 15:2
o Kum 9:18
p Kut 33:14
q Kut 32:9
Kut 33:3
r Hes 14:19
s Zb 33:12
Zb 94:14

Safu ya 2

a 1Sa 12:16
2Sa 7:23
1Nya 17:21
Zb 147:20
b Kut 33:16
Kum 10:21
Isa 64:3
c Kut 19:5
Kum 12:28
d Mwa 15:18
Kut 3:8
Kut 33:2
Kum 7:1
e Kut 23:32
Kum 7:2
Amu 2:2
f Kut 23:33
Yos 23:13
g Kut 23:24
Kum 12:3
Amu 6:25
2Fa 18:4
h Kut 20:3
1Ko 10:14
1Yo 5:21
i Yos 24:19
Eze 39:25
1Ko 10:22
j Law 17:7
Kum 31:16
Amu 2:17
Amu 8:33
Yer 3:9
Eze 6:9
k Hes 25:2
1Ko 10:20

agano: Mbele ya watu wako
wote nitafanya mambo ya ajabu
ambayo hayajapata kuumbwa
kamwe katika dunia yote
wala kati ya mataifa yote;[a] na
watu wote ambao unakaa ka-
tikati yao kwa kweli wataiona
kazi ya Yehova, kwa sababu ni
jambo lenye kuogopesha amba-
lo ninakutendea.[b]
11 "Wewe kwa upande wako
shika ninalokuamuru leo.[c] Ta-
zama, ninawafukuza toka mbe-
le yako Waamori na Wakanaani
na Wahiti na Waperizi na Wahi-
vi na Wayebusi.[d] **12** Jiangalie
usije ukafanya agano pamoja
na wakaaji wa nchi hiyo una-
yoiendea,[e] isije ikawa mtego
katikati yako.[f] **13** Lakini ma-
dhabahu zao mtazibomoa, nazo
nguzo zao takatifu mtazivunja,
nayo miti yao mitakatifu mta-
ikata.[g] **14** Kwa maana huta-
msujudia mungu mwingine,[h]
kwa sababu Yehova, ambaye
jina lake ni Wivu, yeye ni Mu-
ngu mwenye wivu;[i] **15** usije
ukafanya agano na wakaaji wa
nchi hiyo, kwa maana hakika
watafanya uasherati na miu-
ngu[j] yao na kutolea miungu yao
dhabihu,[k] na mtu fulani hakika
atakualika, nawe hakika uta-
kula sehemu ya dhabihu yake.[l]
16 Ndipo utakapolazimika ku-
wachukua baadhi ya binti zao
kwa ajili ya wana wako,[m] na bi-
nti zao hakika watafanya ua-
sherati na miungu yao na ku-
wafanya wana wako wafanye
uasherati na miungu yao.[n]
17 "Usijifanyie miungu ya
sanamu ya kuyeyushwa.[o]
18 "Sherehe ya keki zisizo
na chachu utaishika.[p] Utaku-
la keki zisizo na chachu, kama

---

l Zb 106:28; Eze 18:6; 2Ko 6:14; Ufu 2:20; **m** Ezr 9:2; **n** Hes 25:2; Kum 7:4; 1Fa 11:2; Ne 13:26; **o** Kut 32:8; Law 19:4; **p** Law 23:6; 1Ko 5:8.

vile nilivyokuamuru, siku saba
kwenye ule wakati uliowekwa
katika mwezi wa Abibu,[a] kwa
sababu ni katika mwezi wa Abi-
bu kwamba ulitoka Misri.

19 "Kila kitu ambacho kina-
fungua kwanza tumbo la uza-
zi ni changu,[b] nayo mifugo yako
yote, mzaliwa wa kwanza wa
ng'ombe-dume na wa kondoo.[c]
20 Naye mzaliwa wa kwanza
wa punda utamkomboa kwa ko-
ndoo.[d] Lakini ikiwa hutamko-
mboa, basi utamvunja shingo
yake. Kila mzaliwa wa kwanza
wa wana wako utamkomboa.[e]
Nao wasionekane mbele zangu
mikono mitupu.[f]

21 "Siku sita utafanya kazi,
bali siku ya saba utaishika saba-
to.[g] Wakati wa kulima na waka-
ti wa kuvuna utaishika sabato.[h]

22 "Nawe utaiendeleza she-
rehe yako ya majuma kwa ma-
tunda ya kwanza yaliyoiva ya
mavuno ya ngano,[i] na sherehe
ya kukusanya mwishoni mwa
mwaka.[j]

23 "Mara tatu katika mwa-
ka kila mwanamume wa kwa-
ko ataonekana[k] mbele za Bwa-
na wa kweli, Yehova, Mungu
wa Israeli. **24** Kwa maana ni-
tayafukuzia mbali mataifa toka
mbele yako,[l] nami nitalipanua
eneo lako;[m] wala hakuna mtu
yeyote atakayeitamani nchi
yako wakati utakapokuwa uki-
enda kuuona uso wa Yehova
Mungu wako mara tatu kwa
mwaka.[n]

25 "Usichinje, pamoja na
kitu kilicho na chachu, damu
ya dhabihu yangu.[o] Nayo dhabi-
hu ya sherehe ya pasaka isikae
usiku kucha mpaka asubuhi.[p]

26 "Matunda ya kwanza ya-
liyoiva yaliyo bora[q] zaidi ya
udongo wako utayaleta kwe-
nye nyumba ya Yehova Mungu
wako.[a]

"Usimtokose mwana-mbuzi
katika maziwa ya mama yake."[b]

27 Naye Yehova akaendelea
kumwambia Musa: "Jiandikie
maneno haya,[c] kwa sababu ni-
nafanya agano pamoja nawe
na Israeli kupatana na mane-
no haya."[d] **28** Naye akaende-
lea kuwa huko pamoja na Yeho-
va siku 40, mchana na usiku.
Hakula mkate wala hakunywa
maji.[e] Naye akaandika juu ya
yale mabamba maneno ya lile
agano, yale Maneno Kumi.[f]

29 Sasa ikawa kwamba
Musa alipoteremka kutoka ka-
tika Mlima Sinai, yale maba-
mba mawili ya Ushuhuda yali-
kuwa mkononi mwa Musa ali-
poshuka kutoka mlimani,[g] naye
Musa hakujua kwamba ngozi
ya uso wake ilikuwa ikitoa miale
kwa sababu alikuwa amesema naye.[h] **30** Haruni na wana
wote wa Israeli walipomwona
Musa, lo, tazama! ngozi ya uso
wake ilitoa miale nao wakaogo-
pa kumkaribia.[i]

31 Naye Musa akawaita.
Basi Haruni na wakuu wote
katikati ya kusanyiko wakaru-
di kwake, na Musa akaanza ku-
sema nao. **32** Mara baada ya
hapo wana wote wa Israeli wa-
kamkaribia, naye akaanza ku-
waamuru mambo yote ambayo
Yehova alikuwa amesema naye
juu ya Mlima Sinai.[j] **33** Musa
alipomaliza kusema nao, aliku-
wa akiweka utaji juu ya uso
wake.[k] **34** Lakini Musa ali-
pokuwa akiingia ndani mbele
za Yehova kusema naye, aliku-
wa akiutoa utaji mpaka waka-
ti wa kutoka kwake nje.[l] Naye
akatoka nje na kusema na wana
wa Israeli mambo aliyokuwa

SURA 34
a Kut 23:15
b Kut 13:2
Lu 2:23
c Kut 22:30
d Kut 13:13
e Kut 13:15
Hes 18:15
Hes 18:16
f Kum 16:16
g Kum 5:12
Mt 12:8
Lu 13:14
h Yer 17:22
i Kut 23:16
j Law 23:34
k Kum 16:16
l Kut 34:11
Yos 24:8
m Kum 12:20
Zb 78:55
n Mwa 35:5
Met 16:7
o Kut 23:18
p Kut 12:10
Hes 9:12
q Hes 18:12
Ro 8:23
1Ko 15:23
Yak 1:18
Ufu 14:4

Safu ya 2
a Kum 26:2
Ne 10:35
Met 3:9
Eze 44:30
b Kut 23:19
Kum 14:21
c Kut 24:4
Kum 31:9
Kum 31:11
d Kut 24:8
Kum 4:13
e Kum 9:18
Mt 4:2
f Kut 31:18
Kum 10:2
2Ko 3:6
g Kut 32:15
2Ko 3:3
Ebr 9:4
h Mt 17:2
i 2Ko 3:7
j Kut 24:3
Kum 1:3
k 2Ko 3:13
l 2Ko 3:16

akiamriwa.[a] **35** Nao wana wa
Israeli wakauona uso wa Musa,
kwamba ngozi ya uso wa Musa
ilitoa miale;[b] naye Musa aka-
urudisha utaji juu ya uso wake
mpaka alipoingia ndani kusema naye.[c]

35 Baadaye Musa akaita ku-
sanyiko lote la wana wa
Israeli na kuwaambia: "Haya
ndiyo maneno ambayo Yehova
ameamuru yafanywe:[d] **2** Siku
sita kazi inaweza kufanywa,[e] la-
kini siku ya saba itakuwa kitu
kitakatifu kwenu, sabato ya
pumziko kamili kwa Yehova.
Mtu yeyote anayefanya kazi
siku hiyo atauawa.[f] **3** Msiwa-
she moto katika makao yenu
yoyote katika siku ya sabato."

4 Naye Musa akaendelea ku-
sema na kusanyiko lote la wana
wa Israeli: "Hili ndilo neno
ambalo Yehova ameamuru, na
kusema, **5** 'Kutoka katikati
yenu toeni mchango kwa ajili
ya Yehova.[g] Kila mtu mwenye
moyo wenye nia[h] na aulete uki-
wa mchango wa Yehova, yaa-
ni, dhahabu na fedha na sha-
ba[i] **6** na uzi wa bluu na sufu
iliyotiwa rangi ya zambarau na
kitambaa chenye rangi nyeku-
ndu ya kochinili na kitani bora
na manyoya ya mbuzi[j] **7** na
ngozi za kondoo-dume zilizoti-
wa rangi nyekundu na ngozi za
sili na mbao za mshita **8** na
mafuta kwa ajili ya mwanga
na mafuta ya zeri kwa ajili
ya mafuta yanayotumiwa ku-
tia mafuta na kwa ajili ya uvu-
mba uliotiwa manukato[k] **9** na
mawe ya shohamu na mawe
ya kupamba kwa ajili ya efodi[l]
na kwa ajili ya kifuko cha ki-
fuani.[m]

10 "'Na wote wenye moyo
wa hekima[n] katikati yenu na

SURA 34
a Kum 27:10
b 2Ko 3:7
c 2Ko 3:13

SURA 35
d Kut 34:32
Ro 2:13
Yak 1:22
e Kut 20:9
Kut 31:15
Law 23:3
Kum 5:13
Lu 13:14
f Kut 31:14
Hes 15:32
Hes 15:35
g Kut 35:29
h 2Ko 8:12
2Ko 9:7
i Kut 25:3
j Kut 25:4
Kut 26:7
Kut 36:8
k Kut 25:6
Zb 141:2
Ufu 5:8
l Kut 28:9
Kut 39:14
m Kut 28:15
n Kut 31:6
Kut 36:1

Safu ya 2
a Kut 25:10
b Kut 25:13
c Kut 25:17
d Kut 26:31
e Kut 25:23
f Kut 25:30
Law 24:5
g Kut 25:31
h Kut 27:20
i Kut 30:1
Kut 37:25
Kut 40:5
Zb 141:2
Ufu 5:8
j Kut 30:34
k Kut 27:1
l Kut 30:18
Kut 38:8
m Kut 27:9
n Kut 27:19
o Kut 31:10
Kut 39:41
p Kut 39:1
q Kut 25:2
Kut 36:2
2Ko 8:12
2Ko 9:7

waje na kufanya yote ambayo
Yehova ameamuru, **11** yaa-
ni, ile maskani pamoja na hema
lake na kifuniko chake, kula-
bu zake na mbao zake za viu-
nzi, miti yake, nguzo zake na vi-
kalio vyake; **12** lile Sanduku[a]
na miti[b] yake, kifuniko[c] na pa-
zia[d] la kisitiri; **13** ile meza[e]
na miti yake na vyombo vyake
vyote na mkate wa wonyesho;[f]
14 na kile kinara cha taa[g] cha
kuangaza na vyombo vyake na
taa zake na yale mafuta[h] ya ku-
angaza; **15** na ile madhabahu
ya uvumba[i] na miti yake; na
yale mafuta yanayotumiwa ku-
tia mafuta na ule uvumba uli-
otiwa manukato;[j] na kile kisi-
tiri cha mwingilio kwa ajili ya
mwingilio wa maskani; **16** ile
madhabahu[k] ya toleo la kute-
ketezwa na kile kiunzi cha sha-
ba kwa ajili yake, miti yake na
vyombo vyake vyote; ile bese-
ni[l] na kinara chake; **17** yale
mapazia ya ua,[m] nguzo zake
na vikalio vyake; na kile kisiti-
ri cha lango la ua; **18** ile mi-
sumari ya hema la maskani na
ile misumari ya hema la ua na
kamba zake;[n] **19** yale mavazi[o]
yaliyofumwa kwa ajili ya ku-
hudumu katika patakatifu, yale
mavazi matakatifu[p] kwa ajili ya
Haruni kuhani na yale mavazi
ya wanawe kwa ajili ya kutenda
wakiwa makuhani.'"

20 Basi kusanyiko lote la
wana wa Israeli likaondoka
mbele ya Musa. **21** Kisha wa-
kaja, kila mtu ambaye moyo
wake ulimsukuma,[q] nao wa-
kaleta, kila mtu ambaye roho
yake ilimchochea, mchango wa
Yehova kwa ajili ya kazi ya
hema la mkutano na kwa ajili
ya utumishi wake wote na kwa
ajili ya yale mavazi matakatifu.

22 Nao wakaendelea kuja, wanaume pamoja na wanawake,
kila mtu mwenye moyo wenye
nia. Wakaleta bizimu na vipu-
li na pete na mapambo ya kike,
aina zote za vyombo vya dha-
habu, yaani, kila mtu aliyemto-
lea Yehova toleo la kutikisa la
dhahabu.[a] **23** Na wote walio-
kuwa na uzi wa bluu na sufu
iliyotiwa rangi ya zambarau na
kitambaa chenye rangi nyeku-
ndu ya kochinili na kitani bora
na manyoya ya mbuzi na ngozi
za kondoo-dume zilizotiwa ra-
ngi nyekundu na ngozi za sili,
wakaleta.[b] **24** Wale wote wa-
naochanga mchango wa fedha
na shaba wakaleta mchango
wa Yehova, nao wale wote walio-
kuwa na mbao za mshita kwa
ajili ya kazi yote ya utumishi
wakazileta.

25 Na wanawake wote walio-
kuwa wenye hekima ya moyo[c]
wakasokota kwa mikono yao,
nao wakawa wakileta nyuzi zi-
lizosokotwa za ule uzi wa bluu
na ile sufu iliyotiwa rangi ya za-
mbarau, kile kitambaa chenye
rangi nyekundu ya kochinili na
kile kitani bora. **26** Na wana-
wake wote ambao mioyo yao ili-
wasukuma kwa hekima waka-
sokota manyoya ya mbuzi.

27 Nao wakuu wakaleta
mawe ya shohamu na mawe ya
mapambo kwa ajili ya ile efo-
di na kile kifuko cha kifuani,[d]
28 na yale mafuta ya zeri na yale
mafuta ya kuangaza na ya ku-
tia mafuta na ya uvumba ulio-
tiwa manukato.[e] **29** Kila mwa-
namume na kila mwanamke
ambao mioyo yao iliwachochea
kuleta kitu fulani kwa ajili ya
kazi yote ambayo Yehova ali-
kuwa ameamuru ifanywe kupi-
tia kwa Musa akafanya hivyo;

SURA 35

a Kut 38:24

b Kut 25:4

c Kut 28:3
Kut 31:6
Kut 36:8

d Kut 28:15
Kut 28:29
Kut 28:30
Kut 39:15
Kut 39:21

e Kut 30:23
Kut 30:34

Safu ya 2

a Kut 36:5
Ezr 2:68
2Ko 9:7

b Kut 31:2

c Kut 31:4

d Kut 31:5

e Kut 31:6
Kut 36:1

f Kut 31:3

g Kut 26:1

SURA 36

h Kut 31:6

i 1Fa 4:29
Met 2:6
2Pe 3:15

j Ayu 32:8

k Kut 25:9
Kut 39:1

l Kut 28:3
Kut 31:6
Kut 35:10

m Kut 35:21
Kut 35:26

n Kut 35:5
Met 3:9
2Ko 9:7

wana wa Israeli wakaleta toleo
la hiari kwa Yehova.[a]

30 Kisha Musa akawaambia
wana wa Israeli: "Tazama, Ye-
hova amemwita kwa jina Be-
zaleli[b] mwana wa Uri mwana
wa Huru wa kabila la Yuda.
31 Naye akamjaza roho ya Mu-
ngu katika hekima, katika uele-
waji na katika ujuzi na katika
kila aina ya ufundi **32** na kwa
ajili ya kubuni vyombo, kwa aji-
li ya kazi ya dhahabu na fedha
na shaba,[c] **33** na katika kazi
ya mawe ya kupambia na kati-
ka kazi ya mbao ili kufanya vi-
faa sanifu vya kila namna.[d]
34 Naye ametia moyoni mwa-
ke apate kufundisha, yeye na
Oholiabu[e] mwana wa Ahisama-
ki wa kabila la Dani. **35** Ame-
wajaza hekima ya moyo[f] ili ku-
fanya kazi yote ya fundi na ya
mtarizi[g] na ya mfumaji wa uzi
wa bluu na sufu iliyotiwa rangi
ya zambarau, wa kitambaa che-
nye rangi nyekundu ya kochini-
li na kitani bora, na ya mfuma-
ji wa nguo, watu wanaofanya
kila namna ya kazi na kubuni
vyombo.

36 "Na Bezaleli atafanya
kazi, pia Oholiabu[h] na
kila mtu mwenye moyo wa he-
kima ambaye Yehova amempa
hekima[i] na uelewaji[j] wa mambo
haya ili kujua jinsi ya kufanya
kazi yote ya utumishi mtaka-
tifu kulingana na yote ambayo
Yehova ameamuru."[k]

2 Naye Musa akawaita Be-
zaleli na Oholiabu na kila
mtu mwenye moyo wa hekima
ambaye Yehova alikuwa ame-
tia hekima[l] moyoni mwake,
kila mtu ambaye moyo wake
ulimsukuma kwenda kufanya
kazi.[m] **3** Kisha wakachukua
toka mbele ya Musa michango[n]

yote ambayo wana wa Israeli
walikuwa wameleta kwa ajili ya
kazi ya utumishi mtakatifu ili
kuifanya, na, hao wa mwisho,
bado walimletea matoleo ya hi-
ari asubuhi kwa asubuhi.
4 Na wote wenye hekima wa-
liokuwa wakiifanya kazi yote
takatifu wakaanza kuja, mtu
mmoja baada ya mwingine, ku-
toka katika kazi yao waliyoku-
wa wakiifanya, **5** na kumwa-
mbia Musa: "Watu wanaleta
vitu vingi zaidi kuliko vinavyo-
hitajiwa kwa utumishi kwa aji-
li ya kazi ambayo Yehova ame-
amuru ifanywe." **6** Basi Musa
akaamuru kwamba tangazo li-
tolewe kambini, na kusema:
"Wanaume na wanawake, msi-
toe vitu zaidi kwa ajili ya mcha-
ngo mtakatifu." Basi watu wa-
kazuiliwa wasilete. **7** Navyo
vitu hivyo vikawa vya kutosha
kwa ajili ya kazi yote iliyopasa
kufanywa, na kuzidi.
8 Na wote wenye moyo wa
hekima[a] kati ya wale walioku-
wa wakifanya kazi hiyo wakai-
fanya maskani,[b] vile vitambaa
kumi vya mahema vya kitani
bora kilichosokotwa na uzi wa
bluu na sufu iliyotiwa rangi
ya zambarau na kitambaa che-
nye rangi nyekundu ya kochini-
li; pamoja na makerubi, kazi ya
mtarizi, akavifanya. **9** Urefu
wa kila kitambaa cha hema uli-
kuwa mikono 28, nao upana wa
kila kitambaa ulikuwa mikono
4. Vitambaa vyote hivyo viliku-
wa na kipimo kimoja. **10** Ki-
sha akaunganisha vitambaa vi-
tano pamoja,[c] na vile vitambaa
vingine vitano akaviunganisha
pamoja. **11** Kisha akafanya
vitanzi vya uzi wa bluu kwe-
nye upindo wa kitambaa kili-
cho mahali pa kuungania. Aka-

SURA 36
a Kut 31:6
b Kut 25:9
Kut 39:32
Ebr 9:9
c Kut 26:3

Safu ya 2
a Kut 26:4
b Kut 26:5
c Kut 26:6
Ebr 8:5
Ebr 9:9
d Kut 25:4
Kut 26:7
e Kut 26:8
f Kut 26:9
g Kut 26:10
h Kut 26:11
i Kut 25:5
j Kut 26:14
k Kut 25:10
Kut 25:23
Kut 26:15
Kut 27:1
Kut 30:5
Kut 36:36

fanya vivyo hivyo kwenye upi-
ndo wa kitambaa cha nje kabi-
sa kilicho mahali pale pengine
pa kuungania.[a] **12** Akafanya
vitanzi 50 kwenye kitambaa ki-
moja, akafanya vitanzi 50 kwe-
nye mwisho wa kitambaa kili-
chokuwa mahali pale pengine
pa kuungania, vitanzi hivyo vi-
kiwa vinaelekeana.[b] **13** Mwi-
showe akafanya kulabu 50 za
dhahabu na kuviunganisha vi-
tambaa hivyo pamoja kwa ku-
labu hizo, hivi kwamba hiyo
ikawa maskani moja.[c]
14 Naye akafanya vitambaa
vya mahema vya manyoya ya
mbuzi kwa ajili ya hema lililo
juu ya maskani. Vitambaa kumi
na moja ndivyo alivyofanyi-
za.[d] **15** Urefu wa kila kita-
mbaa ulikuwa mikono 30, nao
upana wa kila kitambaa uliku-
wa mikono 4. Vitambaa hi-
vyo 11 vilikuwa na kipimo ki-
moja.[e] **16** Kisha akaunganis-
ha vitambaa vitano pamoja na
vile vitambaa vingine sita pa-
moja.[f] **17** Kisha akafanya vi-
tanzi 50 kwenye upindo wa ki-
tambaa cha nje kabisa kilicho
mahali pa kuungania, naye aka-
fanya vitanzi 50 kwenye upi-
ndo wa kile kitambaa kingine
kilichoungana nacho.[g] **18** Ki-
sha akafanya kulabu 50 za sha-
ba kwa ajili ya kuliunganisha
hilo hema pamoja liwe kipande
kimoja.[h]
19 Naye akafanya kifuniko
cha hema kutokana na ngozi
za kondoo-dume zilizotiwa ra-
ngi nyekundu na kifuniko ku-
tokana na ngozi za sili,[i] upande
wa juu.[j]
20 Kisha akafanya viunzi
vya mbao vya maskani kuto-
kana na mbao za mshita,[k] vili-
vyosimama upande wa mwisho.

21 Urefu wa kiunzi ulikuwa
mikono kumi, nao upana wa
kila kiunzi ulikuwa mkono
mmoja na nusu.[a] **22** Kila kiu-
nzi kilikuwa na ndimi mbi-
li zilizounganishwa. Hivyo ndi-
vyo alivyofanya viunzi vyote
vya maskani.[b] **23** Basi akafa-
nya viunzi vya maskani, viu-
nzi 20 kwa ajili ya upande una-
oikabili Negebu, kuelekea ku-
sini.[c] **24** Naye akafanya vika-
lio 40 vya fedha viwe chini
ya vile viunzi 20, vikalio viwi-
li chini ya kiunzi kimoja pamo-
ja na ndimi zake mbili na vika-
lio vingine viwili chini ya kiunzi
kingine pamoja na ndimi zake
mbili.[d] **25** Na kwa ajili ya ule
upande mwingine wa maskani,
upande wa kaskazini, akafanya
viunzi 20[e] **26** na vikalio vya-
ke 40 vya fedha, vikalio viwi-
li chini ya kiunzi kimoja na vi-
kalio viwili chini ya kiunzi ki-
ngine.[f]

27 Na kwa ajili ya zile pa-
nde za nyuma za maskani kue-
lekea magharibi akafanya viu-
nzi sita.[g] **28** Naye akafanya
viunzi viwili viwe miimo ya
pembeni ya maskani kwenye
pande zake mbili za nyuma.[h]
29 Nayo ilikuwa pacha upa-
nde wa chini nayo ikawa pacha
mpaka juu ya kila moja kwenye
pete ya kwanza. Hivyo ndivyo
alivyoifanya yote miwili, ile mi-
imo ya pembeni.[i] **30** Basi vi-
kajumlika kuwa viunzi vinane
na vikalio vyake kumi na sita
vya fedha, vikalio viwili kando
ya vikalio viwili chini ya kila ki-
unzi.[j]

31 Naye akafanya miti ya
mshita, mitano kwa ajili ya viu-
nzi vya upande mmoja wa ma-
skani[k] **32** na miti mitano kwa
ajili ya viunzi vya upande ule
mwingine wa maskani na miti
mitano kwa ajili ya viunzi vya
maskani kwa ajili ya zile pande
mbili za nyuma za magharibi.[a]
33 Kisha akafanya mti wa kati-
kati upitie katikati ya vile viu-
nzi toka mwisho mmoja mpaka
ule mwingine.[b] **34** Naye aka-
vifunika vile viunzi kwa dha-
habu, akafanyiza pete zake
za dhahabu ziwe vitegemezo
kwa ajili ya ile miti, akaifunika
ile miti kwa dhahabu.[c]

35 Naye akafanya pazia[d] la
uzi wa bluu na sufu iliyoti-
wa rangi ya zambarau na kita-
mbaa cha rangi nyekundu ya
kochinili na kitani bora kili-
chosokotwa. Akalitia makerubi
kwa kazi ya mtarizi.[e] **36** Ki-
sha akalifanyia nguzo nne za
mshita na kuzifunika kwa dha-
habu, vibanio vyake vikiwa vya
dhahabu, na kutengeneza vi-
kalio vinne vya fedha kwa aji-
li yake.[f] **37** Naye akafanya ki-
sitiri kwa ajili ya mwingilio wa
hema kutokana na uzi wa bluu
na sufu iliyotiwa rangi ya za-
mbarau na kitambaa chenye
rangi nyekundu ya kochinili
na kitani bora kilichosokotwa,
kazi ya mfumaji,[g] **38** na ngu-
zo zake tano na vibanio vyake.
Naye akavifunika vilele vyake
na viungo vyake kwa dhahabu,
lakini vile vikalio vyake vitano
vilikuwa vya shaba.[h]

37 Sasa Bezaleli[i] akafanya
Sanduku[j] la mbao za
mshita. Mikono miwili na nusu
urefu wake, na mkono mmoja
na nusu upana wake, na mko-
no mmoja na nusu kimo chake.[k]
2 Kisha akalifunika kwa dha-
habu safi ndani na nje na kuli-
fanyia ukingo wa dhahabu ku-
lizunguka pande zote.[l] **3** Ki-
sha akalitengenezea pete nne
za dhahabu, za juu ya miguu

SURA 36
a Kut 26:16
b Kut 26:17
c Kut 26:18
d Kut 26:19
e Kut 26:20
f Kut 26:21
g Kut 26:22
h Kut 26:23
i Kut 26:24
j Kut 26:25
k Kut 26:26

Safu ya 2
a Kut 26:27
b Kut 26:28
c Kut 26:29
d Kut 26:31
Kut 40:21
Ebr 10:20
e Mwa 3:24
f Kut 26:32
g Kut 26:36
h Kut 26:37

SURA 37
i Kut 31:2
Kut 38:22
j Kut 40:3
Hes 10:33
k Kut 25:10
l Kut 25:11
Ebr 9:4

yake minne, pete mbili upande
wake mmoja na pete mbili upa-
nde wake mwingine.[a] **4** Kisha
akafanya miti ya mshita na ku-
ifunika kwa dhahabu.[b] **5** Ha-
lafu akaitia miti hiyo kwenye
zile pete zilizo pande za Sandu-
ku ili kulibeba Sanduku.[c]

6 Naye akafanya kifuniko[d]
cha dhahabu safi. Mikono mi-
wili na nusu urefu wake, na
mkono mmoja na nusu upa-
na wake.[e] **7** Kisha akafanya
makerubi wawili wa dhahabu.
Kwa kazi ya kufua akawafa-
nya kwenye miisho yote miwili
ya kifuniko.[f] **8** Kerubi mmo-
ja kwenye mwisho ule, na yule
kerubi mwingine kwenye mwi-
sho huu. Aliwafanya makerubi
juu ya kifuniko kwenye miisho
yote miwili.[g] **9** Nao wakawa
makerubi wanaonyoosha ma-
bawa yao mawili kuelekea juu,
wakisitiri kifuniko kwa maba-
wa yao,[h] nazo nyuso zao zaliku-
wa zikielekeana. Nyuso za ma-
kerubi hao zilielekea kifuniko
hicho.[i]

10 Naye akafanya meza ya
mbao za mshita.[j] Mikono miwi-
li urefu wake, na mkono mmoja
upana wake, na mkono mmoja
na nusu kimo chake.[k] **11** Ha-
lafu akaifunika kwa dhahabu
safi na kufanya ukingo wa dha-
habu kuizunguka pande zote.[l]
12 Kisha akafanya mzingo wa
upana wa kiganja kuizunguka
na kufanya ukingo wa dhahabu
kwa ajili ya mzingo wake kuizu-
nguka pande zote.[m] **13** Tena,
akatengeneza pete nne za dha-
habu kwa ajili yake na kuzi-
weka pete hizo kwenye zile pe-
mbe nne zilizokuwa kwa ajili
ya ile miguu minne.[n] **14** Pete
hizo zilikuwa karibu na ule mzi-
ngo, ili kutegemeza ile miti ya
kuibeba meza hiyo.[a] **15** Hala-
fu akafanya ile miti ya mshi-
ta na kuifunika kwa dhahabu
ili kuibeba ile meza.[b] **16** Baa-
da ya hilo akafanya kutokana
na dhahabu safi vile vyombo vi-
livyo juu ya meza, sahani zake
na vikombe vyake na mabaku-
li yake na mitungi yake iliyotu-
miwa kumimina matoleo ya ki-
nywaji.[c]

17 Kisha akafanya kinara
cha taa[d] cha dhahabu safi. Kwa
kazi ya kufua akakifanya ki-
nara cha taa. Pande zake na
matawi yake, vikombe vyake,
mafundo yake na maua yake vi-
katokea kwake.[e] **18** Na mata-
wi sita yalikuwa yakitoka kwe-
nye pande zake, matawi mata-
tu ya kinara cha taa kutoka
kwenye upande wake mmo-
ja na matawi mengine matatu
ya kinara cha taa kutoka kwe-
nye ule upande wake mwingi-
ne.[f] **19** Vikombe vitatu vye-
nye umbo la maua ya mlozi vi-
likuwa kwenye kikundi kimoja
cha matawi, vifundo na maua
yakifuatana; na vikombe vitatu
vyenye umbo la maua ya mlo-
zi vilikuwa kwenye kile kiku-
ndi kingine cha matawi, vifu-
ndo na maua yakifuatana. Hi-
vyo ndivyo ilivyokuwa kwa
yale matawi sita yaliyokuwa
yakitoka katika kile kinara
cha taa.[g] **20** Na kwenye kile
kinara cha taa kulikuwa na
vikombe vinne vyenye umbo
la maua ya mlozi, vifundo vya-
ke na maua yake yakifuatana.[h]
21 Na kile kifundo chini ya ma-
tawi mawili kilitoka kwake, na
kifundo kilicho chini ya yale
matawi mengine mawili kilito-
ka kwake, na kifundo kingine
kilicho chini ya matawi mengi-
ne mawili zaidi kilitoka kwake,

SURA 37

a Kut 25:12

b Kut 25:13
2Nya 5:9

c Kut 25:14
Yos 3:8

d Law 16:2
Law 16:14
1Nya 28:11

e Kut 25:17

f Kut 25:18
Kut 40:20

g Kut 25:19

h Mwa 3:24
Kut 25:20
Ebr 9:5

i 1Sa 4:4
Zb 80:1

j Kut 35:13
Kut 40:4

k Kut 25:23

l Kut 25:24

m Kut 25:25

n Kut 25:26

Safu ya 2

a Kut 25:27

b Kut 25:28

c Kut 25:29
Yer 52:19

d Kut 40:24
Law 24:4
2Nya 13:11

e Kut 25:31

f Kut 25:32

g Kut 25:33

h Kut 25:34

kwa ajili ya matawi sita yanayotoka katika kinara.[a] **22** Vifundo vyake na matawi yake
vilitoka kwake. Vyote vilikuwa kitu kimoja cha kazi ya ku-
fua, cha dhahabu safi.[b] **23** Kisha akafanya taa zake saba na
mikasi ya tambi zake na vyetezo vyake kutokana na dhahabu
safi.[c] **24** Alikifanya kwa talanta ya dhahabu safi, hicho pa-
moja na vyombo vyake vyote.

25 Sasa akafanya madhabahu ya uvumba[d] kutokana na
mbao za mshita.[e] Mkono mmoja urefu wake na mkono mmo-
ja upana wake, ikiwa mraba, na mikono miwili kimo cha-
ke. Pembe zake zilitoka kwake.[f] **26** Kisha akaifunika kwa dha-
habu safi, upande wake wa juu na pande zake za kando kui-
zunguka na pembe zake, naye akafanya ukingo wa dha-
habu kuizunguka pande zote.[g] **27** Naye akaifanyia pete mbili
za dhahabu chini ya ukingo wake kwenye pande zake mbi-
li, kwenye pande zake mbili zinazoelekeana, za kutegeme-
za ile miti ya kuibeba.[h] **28** Kisha akafanya ile miti ya mshi-
ta na kuifunika kwa dhahabu.[i] **29** Tena akafanya yale mafu-
ta yanayotumiwa kutia mafuta[j] na ule uvumba safi uliotiwa
manukato,[k] kazi ya mtengenezaji wa marhamu.

38 Naye akafanya madhabahu ya toleo la kuteketezwa kwa mbao za mshita.
Mikono mitano urefu wake, na mikono mitano upana wake, ili-
kuwa mraba, na mikono mitatu kimo chake.[l] **2** Halafu akafa-
nya pembe zake[m] kwenye zile ncha zake nne. Pembe zake zi-
litoka kwake. Kisha akaifunika kwa shaba.[n] **3** Baada ya
hilo akavifanya vyombo vyote vya madhabahu, yale makopo
na zile sepetu na yale mabakuli, zile nyuma na vile vyetezo.
Vyombo vyake vyote alivifanya kwa shaba.[a] **4** Tena akaifanyia
madhabahu kiunzi cha fito, mtandao wa shaba, chini ya
ukingo wake, chini kuelekea katikati yake.[b] **5** Halafu akate-
ngeneza pete nne kwenye ile miisho minne karibu na kile ki-
unzi cha shaba, ili kuitegemeza ile miti. **6** Baada ya hilo aka-
fanya miti ya mshita na kuifunika kwa shaba.[c] **7** Kisha aka-
itia ile miti kwenye zile pete zilizo pande za madhabahu
ili kuibeba.[d] Akaifanya kuwa sanduku la mbao lenye uwazi.[e]

8 Kisha akafanya beseni ya shaba[f] na kinara chake cha sha-
ba, kwa kutumia vioo vya watumishi wanawake ambao wali-
fanya utumishi uliopangwa kwenye mwingilio wa hema la mku-
tano.[g]

9 Naye akafanya ule ua.[h] Upande unaokabili Negebu, ku-
elekea kusini, mapazia ya ua yalikuwa ya kitani bora ki-
lichosokotwa, kwa mikono mia moja.[i] **10** Nguzo zake 20 na vi-
kalio vyake 20 vilikuwa vya shaba. Misumari ya nguzo na
viungo vyake vilikuwa vya fedha.[j] **11** Pia, kwa ajili ya upa-
nde wa kaskazini kulikuwa na mikono 100. Nguzo zake 20
na vikalio vyake 20 vilikuwa vya shaba. Misumari ya nguzo
na viungo vyake vilikuwa vya fedha.[k] **12** Lakini kwa ajili ya
upande wa magharibi mapazia yalikuwa mikono 50. Nguzo
zake zilikuwa 10 na vikalio vyake 10.[l] Misumari ya nguzo na
viungo vyake vilikuwa vya fedha. **13** Na kwa ajili ya upa-

SURA 37
a Kut 25:35
b Kut 25:36
c Kut 25:37
Kut 25:38
Hes 8:2
d Kut 30:7
Kut 39:38
Zb 141:2
Lu 1:10
Ufu 8:3
e Kut 30:1
Kut 40:5
f Kut 30:2
g Kut 30:3
h Kut 30:4
i Kut 30:5
j Kut 30:25
Kut 30:33
Kut 40:9
1Nya 9:30
Zb 45:7
Ebr 1:9
k Kut 30:35
Zb 141:2
Ufu 5:8

SURA 38
l Kut 27:1
Kut 40:10
Ebr 13:10
m Kut 27:2
n 2Nya 1:5

Safu ya 2
a Kut 27:3
b Kut 27:4
c Kut 27:6
d Kut 27:7
e Kut 27:8
f Kut 30:18
Kut 31:9
Kut 40:7
Law 8:11
1Fa 7:23
g 1Sa 2:22
h Kut 40:8
Zb 84:2
Zb 92:13
i Kut 27:9
j Kut 27:10
Hes 3:37
k Kut 27:11
l Kut 27:12

nde wa mashariki kuelekea macheo ya jua kulikuwa na mikono 50.[a] **14** Mapazia yalikuwa mikono kumi na mitano kwa upande mmoja. Nguzo zake zilikuwa tatu na vikalio vyake vitatu.[b] **15** Na kwa ajili ya upande ule mwingine, huu na ule, wa lango la ua, mapazia yalikuwa mikono kumi na mitano. Nguzo zake zilikuwa tatu na vikalio vyake vitatu.[c] **16** Mapazia yote ya ua kuzunguka pande zote yalikuwa ya kitani bora kilichosokotwa. **17** Navyo vikalio vya nguzo vilikuwa vya shaba. Vibanio vya vikalio na viungo vyake vilikuwa vya fedha navyo vilifunikwa kwa shaba sehemu ya juu, na kulikuwa na viungo vya shaba kwa ajili ya nguzo zote za ua.[d]

18 Nacho kisitiri cha lango la ua kilikuwa kazi ya mfumaji, cha uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kitani bora kilichosokotwa,[e] na urefu wake ulikuwa mikono 20, nacho kimo kotekote kilikuwa mikono 5 sawasawa na mapazia ya ua.[f] **19** Na nguzo zake nne na vikalio vyake vinne vilikuwa vya shaba. Misumari yake ilikuwa ya fedha na utando wa vichwa vyake na viungo vyake ulikuwa wa fedha. **20** Na misumari yote ya hema kwa ajili ya maskani na kwa ajili ya ua kuzunguka pande zote ilikuwa ya shaba.[g]

21 Hivi ndivyo vitu vilivyohesabiwa vya maskani, maskani ya Ushuhuda,[h] vilivyohesabiwa kwa amri ya Musa, kuwa utumishi wa Walawi[i] chini ya uongozi wa Ithamari[j] mwana wa Haruni kuhani. **22** Naye Bezaleli[k] mwana wa Uri mwana wa Huru wa kabila la Yuda alifanya yote ambayo Yehova alikuwa amemwamuru Musa. **23** Na pamoja naye alikuwa Oholiabu[a] mwana wa Ahisamaki wa kabila la Dani, fundi na mtarizi na mfumaji wa uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kitani bora.

24 Dhahabu yote iliyotumiwa kwa ajili ya kazi katika kazi yote ya mahali patakatifu ikawa jumla ya dhahabu ya toleo la kutikisa,[b] talanta 29 na shekeli 730 kulingana na shekeli[c] ya mahali patakatifu.[d] **25** Nayo fedha ya wale walioandikishwa kati ya kusanyiko ilikuwa talanta 100 na shekeli 1,775 kulingana na shekeli ya mahali patakatifu. **26** Ile nusu shekeli kwa ajili ya mtu mmoja ilikuwa nusu shekeli kulingana na shekeli ya mahali patakatifu, kwa kila mtu aliyekuwa akipita kuingia upande wa wale waliokuwa wameandikishwa kuanzia miaka 20 na zaidi,[e] jumla ya watu 603,550.[f]

27 Na talanta mia moja za fedha zilitumiwa kutengeneza vikalio vya mahali patakatifu na vikalio vya lile pazia. Vikalio mia moja vilitoshana na talanta mia moja, talanta moja kwa kikalio kimoja.[g] **28** Na kutokana na zile shekeli 1,775 alifanyiza vibanio vya nguzo na kuvifunika sehemu yake ya juu na kuviunganisha pamoja.

29 Nayo shaba ya toleo la kutikisa ilikuwa talanta 70 na shekeli 2,400. **30** Naye akaitumia kufanya vile vikalio vya mwingilio wa hema la mkutano na ile madhabahu ya shaba na kile kiunzi chake cha shaba, na vyombo vyote vya madhabahu,

SURA 38

a Kut 27:13

b Kut 27:14

c Kut 27:15

d Kut 27:17

e Kut 35:6

f Kut 27:16

g Kut 27:19

h Kut 25:16
Kut 31:18
Kut 34:29
Hes 17:7

i Hes 3:6
Hes 4:47

j Kut 6:23
Hes 4:28
1Nya 6:3

k Kut 31:2
Kut 35:30
Kut 36:1
Kut 37:1
2Nya 1:5

Safu ya 2

a Kut 31:6
Kut 35:34
Kut 36:2

b Kut 35:22

c Kut 30:13
Hes 3:47
Hes 18:16

d Law 5:15
Law 27:3

e Kut 30:15

f Kut 12:37
Hes 1:46

g Kut 26:19
Kut 26:25
Kut 26:32

31 na vile vikalio vya ua kuzunguka pande zote, na vile vikalio vya lango la ua, na misumari yote ya maskani na misumari[a] yote ya ua kuzunguka pande zote.

39 Na kutokana na ule uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili[b] wakafanya mavazi[c] yaliyofumwa kwa ajili ya kuhudumu katika mahali patakatifu.[d] Basi wakafanya yale mavazi matakatifu[e] yaliyokuwa kwa ajili ya Haruni, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

2 Basi akaifanya ile efodi[f] ya dhahabu, uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kitani bora kilichosokotwa. **3** Kisha wakafua mabamba ya dhahabu yawe mabamba membamba, naye akakata nyuzi za kufuma pamoja na ule uzi wa bluu na ile sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kile kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kile kitani bora, kama kazi ya mtarizi.[g] **4** Wakaifanyia vipande vya begani vilivyounganishwa. Iliunganishwa kwenye miisho yake miwili. **5** Nao mshipi, uliokuwa juu yake ili kuifunga, ulikuwa wa kitambaa kilekile kulingana na ufundi wake, wa dhahabu, uzi wa bluu, na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kitani bora kilichosokotwa,[h] kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

6 Kisha wakafanya mawe ya shohamu[i] yaliyopangwa kwenye mapambo ya dhahabu, yaliyochongwa kwa michoro ya muhuri kulingana na majina ya wana wa Israeli.[a] **7** Basi akayaweka kwenye vile vipande vya begani vya efodi yawe mawe ya ukumbusho[b] kwa ajili ya wana wa Israeli, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa. **8** Kisha akafanya kile kifuko cha kifuani[c] kwa ufundi wa mtarizi, kama ule ufundi wa efodi, kutokana na dhahabu, uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kitani bora kilichosokotwa.[d] **9** Kilikuwa mraba kilipokunjwa. Walikifanya kile kifuko cha kifuani, kinapokunjwa, shubiri moja urefu wake na shubiri moja upana wake.[e] **10** Kisha wakakijaza kwa mistari minne ya mawe. Mstari wa zabarijadi, topazi na zumaridi ulikuwa mstari wa kwanza.[f] **11** Nao mstari wa pili[g] ulikuwa feruzi, yakuti[h] na yaspi.[i] **12** Nao mstari wa tatu[j] ulikuwa jiwe la *leshemi,* akiki na amethisti. **13** Nao mstari wa nne[k] ulikuwa krisolito na shohamu[l] na yashefi. Yaliwekwa katika mapambo ya dhahabu katika mahali pake. **14** Na mawe hayo yalikuwa kulingana na majina ya wana wa Israeli. Yalikuwa kumi na mawili kulingana na majina yao, kwa michongo ya muhuri, kila moja kulingana na jina lake kwa ajili ya yale makabila kumi na mawili.[m]

15 Nao wakafanya juu ya kile kifuko cha kifuani minyororo yenye mashada, msokoto wa kamba, wa dhahabu safi.[n] **16** Kisha wakafanya mapambo mawili ya dhahabu na pete mbili za dhahabu na kuziweka hizo pete mbili kwenye ile miisho

SURA 38
a Kut 27:19

SURA 39
b Kut 25:4
Kut 35:23
c Kut 29:5
Kut 31:10
Kut 35:19
d Kut 25:8
Law 16:2
e Kut 28:4
f Kut 25:7
Kut 28:6
Law 8:7
g Kut 26:1
Kut 36:8
h Kut 28:8
Kut 29:5
Isa 11:5
i Kut 25:7
Kut 35:9

Safu ya 2
a Kut 1:1
Kut 28:9
Kut 28:10
b Kut 28:12
c Kut 25:7
Law 8:8
d Kut 28:15
e Kut 28:16
f Kut 28:17
g Kut 28:18
h Ayu 28:6
i Ufu 4:3
j Kut 28:19
k Kut 28:20
l Mwa 2:12
1Nya 29:2
m Kut 28:21
n Kut 28:22

miwili ya kile kifuko cha kifuani.[a] **17** Baada ya hilo wakapitisha zile kamba mbili za dhahabu kwenye zile pete mbili zilizo kwenye miisho ya kile kifuko cha kifuani.[b] **18** Nao wakapitisha ile miisho miwili ya zile kamba mbili kwenye yale mapambo mawili. Halafu wakaiweka juu ya vile vipande vya begani vya efodi, mbele yake.[c] **19** Kisha wakafanya pete mbili za dhahabu na kuziweka kwenye ile miisho miwili ya kile kifuko cha kifuani kwenye upindo wake ulio upande unaoelekea ile efodi upande wa ndani.[d] **20** Halafu wakafanya pete mbili za dhahabu na kuziweka juu ya vile vipande viwili vya begani vya efodi upande wake wa chini, sehemu yake ya mbele, karibu na mahali pake pa kuungania, juu ya ule mshipi wa efodi.[e] **21** Mwishowe wakakifunga kile kifuko cha kifuani kwa pete zake kwenye zile pete za efodi kwa uzi wa bluu, ili kipate kuwa juu ya mshipi wa efodi na kile kifuko cha kifuani kisiondoke juu ya efodi, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.[f]

22 Kisha akafanya lile koti lisilo na mikono[g] la efodi, ufundi wa mfumaji, lote la uzi wa bluu. **23** Na sehemu wazi ya hilo koti ilikuwa katikati yake, kama sehemu wazi ya vazi la chuma. Sehemu hiyo iliyo wazi ilikuwa na ukingo kuizunguka pande zote ili isiraruke.[h] **24** Halafu wakafanya kwenye upindo wa hilo koti makomamanga ya uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili, vilivyosokotwa pamoja.[i] **25** Na zaidi, wakafanya kengele za dhahabu safi na kuziweka kengele hizo katikati ya makomamanga[a] kwenye upindo wa lile koti kuzunguka pande zote, katikati ya makomamanga; **26** kengele na komamanga, kengele na komamanga kwenye upindo wa hilo koti kuzunguka pande zote,[b] kwa ajili ya kuhudumu, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

27 Kisha wakafanya zile kamba za kitani bora,[c] ufundi wa mfumaji, kwa ajili ya Haruni na wanawe, **28** na kile kilemba[d] cha kitani bora na yale mavalio ya kichwani[e] ya mapambo ya kitani bora na zile suruali[f] za kitani bora kilichosokotwa, **29** na ule ukumbuu[g] wa kitani bora kilichosokotwa na uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili, kazi ya mfumaji, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

30 Mwishowe wakafanya lile bamba linalong'aa, ishara takatifu ya wakfu, kutokana na dhahabu safi na kuandika juu yake maandishi kwa mchongo wa muhuri: "Utakatifu ni wa Yehova."[h] **31** Kisha wakalitia uzi wa bluu ili waliweke juu ya kile kilemba upande wa juu,[i] kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

32 Basi kazi ya ile maskani ya hema la mkutano ikafikia mwisho wake, kwa maana wana wa Israeli waliendelea kufanya kulingana na yote ambayo Yehova alikuwa amemwamuru Musa.[j] Walifanya vivyo hivyo.

33 Nao wakaileta maskani[k] kwa Musa, lile hema[l] pamoja na vyombo vyake vyote,[m] kulabu[n]

SURA 39

a Kut 28:23

b Kut 28:24

c Kut 28:25

d Kut 28:26

e Kut 28:27

f Kut 28:28

g Kut 28:31
Law 8:7
Isa 61:10

h Kut 28:32

i Kut 28:33

Safu ya 2

a 2Fa 25:17

b Kut 28:34

c Kut 28:39
Law 8:7
Law 8:13
Ufu 19:8

d Kut 28:4
Kut 28:39

e Kut 28:40
Kut 29:9
Law 8:13

f Kut 28:42
Eze 44:18

g Kut 28:4
Kut 28:39
Isa 11:5

h Kut 28:36
Law 8:9
Zek 14:20

i Kut 28:37

j Kut 25:40
Ebr 8:5

k Kut 36:8

l Kut 36:14

m Kut 31:7

n Kut 36:18

zake, viunzi vyake vya mbao,[a]
miti[b] yake na nguzo zake na
vikalio[c] vyake, **34** na kifuni-
ko chake cha ngozi za kondoo-
dume zilizotiwa rangi[d] nyeku-
ndu na kifuniko chake cha
ngozi za sili[e] na pazia la kisi-
tiri,[f] **35** na sanduku[g] la ushu-
huda na miti[h] yake na kifuni-
ko,[i] **36** meza,[j] vyombo vyake
vyote[k] na ule mkate wa wonye-
sho, **37** kile kinara cha taa[l]
cha dhahabu safi, taa zake, ule
mstari wa taa,[m] na vyombo vya-
ke vyote[n] na yale mafuta ya
kuangazia,[o] **38** na madhaba-
hu[p] ya dhahabu na yale mafu-
ta yanayotumiwa kutia mafu-
ta[q] na ule uvumba uliotiwa ma-
nukato[r] na kile kisitiri[s] kwa ajili
ya mwingilio wa hema, **39** ile
madhabahu[t] ya shaba na kile
kiunzi[u] chake cha shaba, miti[v]
yake na vyombo vyake vyo-
te,[w] ile beseni[x] na kinara[y] cha-
ke, **40** mapazia[z] ya ua, nguzo[a]
zake na vikalio[b] vyake na kile
kisitiri[c] kwa ajili ya lango la ua,
kamba[d] zake za hema na misu-
mari[e] yake ya hema na vyombo
vyote[f] kwa ajili ya utumishi wa
maskani, kwa ajili ya hema la
mkutano, **41** yale mavazi[g] ya-
liyofumwa kwa ajili ya kuhu-
dumu katika patakatifu, yale
mavazi matakatifu[h] kwa ajili
ya Haruni kuhani na mavazi ya
wanawe ya kutumikia wakiwa
makuhani.[i]

42 Kulingana na yote amba-
yo Yehova alikuwa amemwa-
muru Musa, hivyo ndivyo wana
wa Israeli walivyoufanya utu-
mishi wote.[j] **43** Naye Musa
akaiona ile kazi yote, na, ta-
zama! walikuwa wameifanya
kama vile Yehova alivyoku-
wa ameamuru. Hivyo ndivyo
walivyokuwa wamefanya. Basi
Musa akawabariki.[k]

SURA 39

a Kut 36:20
b Kut 36:31
c Kut 36:24
d Kut 36:19
e Kut 26:14
f Kut 36:35
g Kut 37:1
h Kut 37:4
i Kut 37:6
j Kut 37:10
k Kut 37:16
l Kut 37:17
m Kut 37:23
n Kut 25:38
o Kut 35:28
p Kut 37:25
q Kut 37:29
r Kut 30:35
s Kut 36:37
t Kut 38:1
u Kut 38:4
v Kut 38:6
w Kut 38:30
x Kut 38:8
y Kut 30:18
z Kut 38:9
a Kut 38:10
b Kut 38:11
c Kut 38:18
d Kut 35:18
e Kut 38:20
f Kut 27:19
g Kut 31:10
h Kut 28:3
i Kut 35:19
j Kut 35:10
Kut 36:1
k Law 9:23
Hes 6:23
Yos 22:6
1Fa 8:14
2Nya 30:27

Safu ya 2

SURA 40

a Kut 12:2
Kut 34:18
Est 3:7
b Hes 7:1
c Kut 25:21
d Hes 4:5
Ebr 9:3
Ebr 10:20
e Kut 26:35
f Kut 25:31
Ebr 9:2
g Kut 25:37
h Kut 30:1
Zb 141:2
Lu 1:10
Ufu 5:8
i Kut 26:36
Kut 39:38
j Kut 38:1
1Ko 10:18
Ebr 13:10
k Kut 30:18
l Kut 27:9
m Kut 27:16
Kut 38:18
n Kut 30:25
Ebr 1:9
o Law 8:10
Hes 7:1
p Kut 29:36
Law 8:11
q Kut 29:37
r Law 8:6
Efe 5:26
Ebr 7:28

40 Kisha Yehova akasema
na Musa, na kumwa-
mbia: **2** "Katika siku ya mwe-
zi wa kwanza,[a] siku ya kwa-
nza ya mwezi, utaisimamisha
maskani ya hema la mkutano.[b]
3 Nawe utaliweka sanduku la
ushuhuda[c] ndani yake na kufu-
nga kwa pazia[d] njia ya kuingia
penye Sanduku. **4** Nawe utai-
leta meza[e] ndani na kuweka
kwa utaratibu mpangilio wake,
nawe utakileta ndani kile kina-
ra cha taa[f] na kuziwasha taa
zake.[g] **5** Nawe utaiweka ma-
dhabahu ya dhahabu kwa ajili
ya uvumba[h] mbele ya sanduku
la ushuhuda na kuweka kile ki-
sitiri cha mwingilio wa maska-
ni mahali pake.[i]

6 "Nawe utaweka ile madha-
bahu[j] ya matoleo ya kuteke-
tezwa mbele ya mwingilio wa
maskani ya hema la mkuta-
no, **7** nawe utaweka ile beseni
katikati ya hema la mkuta-
no na ile madhabahu na kutia
maji ndani yake.[k] **8** nawe uta-
weka ua[l] kuzunguka pande zote
na kuweka kile kisitiri[m] cha la-
ngo la ua. **9** Nawe utachukua
yale mafuta yanayotumiwa ku-
tia mafuta na kuitia mafuta[n]
maskani na vyote vilivyomo
ndani yake,[o] nawe utaitakasa
pamoja na vyombo vyake vyo-
te, nayo itakuwa kitu kitakati-
fu. **10** Nawe utaitia mafuta
madhabahu ya toleo la kuteke-
tezwa na vyombo vyake vyote
na kuitakasa madhabahu[p] hiyo,
nayo itakuwa madhabahu ta-
katifu zaidi.[q] **11** Nawe utaitia
mafuta ile beseni na kinara cha-
ke na kuitakasa.

12 "Kisha utamleta Haruni
na wanawe karibu na mwingi-
lio wa hema la mkutano na ku-
waosha kwa maji.[r] **13** Nawe

utamvisha Haruni mavazi matakatifu[a] na kumtia mafuta[b] na kumtakasa, naye atatenda akiwa kuhani kwangu. **14** Baada ya hilo utawaleta wanawe karibu, nawe utawavika kanzu.[c] **15** Nawe lazima utawatia mafuta kama vile ulivyomtia mafuta baba yao,[d] nao lazima watanitumikia wakiwa makuhani, na kutiwa kwao mafuta lazima kutumike kwao kwa kuendelea kukiwa ukuhani mpaka wakati usio na kipimo katika vizazi vyao."[e]

16 Naye Musa akafanya kulingana na yote ambayo Yehova alikuwa amemwamuru.[f] Alifanya vivyo hivyo.

17 Basi ikawa kwamba katika mwezi wa kwanza, katika mwaka wa pili, siku ya kwanza ya mwezi, maskani ilisimamishwa.[g] **18** Musa alipoisimamisha maskani, aliweka vikalio[h] vyake chini na kuweka viunzi vyake vya mbao[i] na kuweka miti[j] yake na kusimamisha nguzo[k] zake. **19** Halafu akatandaza lile hema[l] juu ya maskani na kuweka kifuniko[m] cha hema juu yake, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

20 Baada ya hilo akachukua ule Ushuhuda[n] na kuuweka katika Sanduku[o] na kuiweka ile miti[p] kwenye lile Sanduku na kuweka kile kifuniko[q] juu ya lile Sanduku.[r] **21** Halafu akaleta lile Sanduku ndani ya maskani na kuweka lile pazia[s] la kusitiri mahali pake na kufunga njia ya kuingia penye sanduku la ushuhuda,[t] kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

22 Kisha akaiweka meza[u] katika lile hema la mkutano upande wa maskani kuelekea kaskazini nje ya lile pazia, **23** naye akapanga mstari wa mikate[a] juu yake mbele za Yehova, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

24 Halafu akaweka kile kinara cha taa[b] ndani ya hema la mkutano mbele ya ile meza, upande wa maskani kuelekea kusini. **25** Kisha akawasha zile taa[c] mbele za Yehova, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

26 Kisha akaweka ile madhabahu ya dhahabu[d] ndani ya hema la mkutano mbele ya lile pazia, **27** ili afukize juu yake uvumba uliotiwa manukato,[e] kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

28 Mwishowe akaweka kile kisitiri[f] cha mwingilio wa maskani mahali pake.

29 Naye akaweka ile madhabahu[g] ya toleo la kuteketezwa kwenye mwingilio wa hema la mkutano, ili atoe juu yake toleo la kuteketezwa[h] na toleo la nafaka, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

30 Halafu akaweka ile beseni kati ya hema la mkutano na ile madhabahu na kutia ndani yake maji ya kuosha.[i] **31** Naye Musa na Haruni na wanawe wakaosha mikono yao na miguu yao hapo. **32** Walipoingia kwenye hema la mkutano na walipoenda karibu na ile madhabahu, walikuwa wakioga,[j] kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

33 Mwishowe akaweka ua[k] kuizunguka pande zote ile maskani na ile madhabahu na kuweka kisitiri cha lango la ua.[l]

Basi Musa akaimaliza kazi. **34** Nalo wingu[m] likaanza kulifunika hema la mkutano, na

SURA 40

a Kut 29:5
Law 8:7
b Law 8:12
Zb 133:2
Mdo 10:38
c Law 8:13
d Law 8:30
2Ko 1:21
e Hes 25:13
Ebr 7:11
Ebr 7:23
f Kut 39:43
Kum 4:2
g Hes 7:1
Hes 9:15
h Kut 36:24
i Kut 26:15
j Kut 36:31
k Kut 35:11
l Kut 26:7
Kut 36:14
m Kut 26:14
n Kut 16:34
Kut 31:18
o Kut 25:22
Kut 37:1
p Kut 37:4
1Fa 8:8
q Kut 37:6
1Nya 28:11
r Law 16:2
s Kut 36:35
Ebr 10:20
t Ebr 9:3
Ebr 10:19
u Kut 37:10
Ebr 9:2

Safu ya 2

a Kut 25:30
Mt 12:4
b Kut 37:17
c Kut 25:37
Kut 37:23
Zb 119:105
d Kut 30:1
Kut 37:25
e Kut 30:7
Kut 30:35
f Kut 26:36
Kut 36:37
g Kut 38:1
Ebr 13:10
h Kut 29:38
i Kut 30:18
Ebr 10:22
j Kut 30:19
k Kut 27:9
Kut 38:9
l Kut 38:18
m Law 16:2
Hes 9:15
Hes 16:42
1Fa 8:10
Ufu 15:8

utukufu wa Yehova ukaijaza maskani. **35** Naye Musa hakuweza kuingia ndani ya hema la mkutano, kwa sababu wingu[a] lilikaa juu yake na utukufu wa Yehova uliijaza maskani.[b]

36 Na wakati ambapo wingu hilo lilikuwa likiinuka kutoka juu ya maskani wana wa Israeli walikuwa wakivunja kambi katika hatua zao zote za safari.[a] **37** Hata hivyo, ikiwa wingu hilo halikuinuka, basi hawakuwa wakivunja kambi mpaka siku ambayo liliinuka.[b] **38** Kwa maana wingu la Yehova lilikuwa juu ya maskani wakati wa mchana, na moto ulikuwa juu yake wakati wa usiku machoni pa nyumba yote ya Israeli katika hatua zao zote za safari.[c]

SURA 40
a Zb 78:14
b Kut 29:43
2Nya 5:14

Safu ya 2
a Hes 10:11
Ne 9:19
b Hes 9:17
Hes 9:22
c Kut 13:21
Hes 9:16
Zb 78:14

MAMBO YA WALAWI

1 Yehova akamwita Musa, akasema naye kutoka katika hema la mkutano,[a] akamwambia: **2** "Sema na wana wa Israeli,[b] nawe utawaambia, 'Ikiwa mtu fulani kati yenu atatoa toleo kwa Yehova kutoka katika wanyama wa kufugwa, mtatoa toleo lenu kutoka katika mifugo na kutoka katika kundi.

3 "'Ikiwa toleo lake ni toleo la kuteketezwa[c] kutoka katika mifugo, atamtoa dume, asiye na kasoro.[d] Atamtoa kwenye mwingilio wa hema la mkutano kwa hiari yake mwenyewe mbele za Yehova.[e] **4** Naye ataweka mkono wake juu ya kichwa cha toleo hilo la kuteketezwa, nalo litakubaliwa[f] kwa neema ili afanye upatanisho kwa ajili yake.[g]

5 "'Kisha yule ng'ombe-dume mchanga atachinjwa mbele za Yehova; na wana wa Haruni, makuhani,[h] wataitoa damu na kuinyunyiza damu hiyo kwenye madhabahu kuizunguka pande zote,[i] madhabahu iliyo kwenye mwingilio wa hema la mkutano. **6** Nalo toleo la kuteketezwa litachunwa ngozi na kukatwa katika vipande vyake.[a] **7** Na wana wa Haruni, makuhani, watawasha moto kwenye madhabahu[b] na kuweka kuni kwa utaratibu kwenye moto.[c] **8** Na wana wa Haruni, makuhani, watavipanga vile vipande[d] kwa utaratibu, kichwa na mafuta juu ya kuni zilizo katika moto ulio kwenye madhabahu. **9** Na matumbo[e] yake na miguu yake itaoshwa kwa maji; naye kuhani atafukiza vyote hivyo kwenye madhabahu viwe toleo la kuteketezwa, toleo linalotolewa kwa njia ya moto lililo na harufu ya kumtuliza Yehova.[f]

10 "'Na ikiwa toleo lake linatoka katika kundi,[g] kutoka kati ya wana-kondoo dume au mbuzi, wa kiume,[h] asiye na kasoro, ndiye atakayemtoa kuwa toleo la kuteketezwa.[i] **11** Naye atachinjwa kando ya madhabahu kuelekea kaskazini mbele za Yehova, nao wana wa Haruni, makuhani, watainyunyiza damu yake kwenye madhabahu pande zote.[j] **12** Naye atamkata katika vipande vyake na ki-

SURA 1
a Kut 40:34
Hes 12:5
b Law 22:18
c Law 12:6
Hes 15:3
d Kut 12:5
Law 22:20
Kum 15:21
Mal 1:14
Ebr 9:14
1Pe 1:19
e 2Ko 9:7
f Isa 56:7
g Hes 15:25
Ro 3:25
1Yo 2:2
h Ebr 10:11
i Ebr 9:13
1Pe 1:2

Safu ya 2
a Law 7:8
b Law 6:12
c Mwa 22:9
Ne 13:31
d Kut 29:17
Law 9:13
1Fa 18:23
e Law 8:21
Law 9:14
f Mwa 8:21
Kut 29:18
Hes 15:3
Efe 5:2
Flp 4:18
g Mwa 4:4
h Law 22:19
i Law 22:20
Mal 1:14
1Pe 1:19
j Law 9:12
2Nya 29:22

chwa chake na mafuta yake,
naye kuhani ataviweka kwa
utaratibu juu ya kuni zilizo
katika moto ulio kwenye ma-
dhabahu.[a] **13** Naye atayaosha
matumbo[b] na miguu[c] kwa maji;
naye kuhani atatoa vyote hivyo
na kuvifukiza[d] kwenye madha-
bahu. Ni toleo la kuteketezwa,
toleo linalotolewa kwa njia ya
moto lililo na harufu ya kumtu-
liza Yehova.[e]

14 "'Hata hivyo, ikiwa toleo
lake la kuteketezwa kwa Yeho-
va ni toleo linalotoka kati ya
ndege, basi atatoa toleo lake
kutoka kati ya njiwa-tetere[f] au
hua wachanga.[g] **15** Naye ku-
hani atamtoa kwenye madha-
bahu na kukikongonyoa[h] ki-
chwa chake na kumfukiza kwe-
nye madhabahu, lakini damu
yake itamwagwa kando ya ma-
dhabahu. **16** Naye ataondoa
gole lake na manyoya yake
na kuyatupa kando ya madha-
bahu, upande wa mashariki,
mahali pa majivu yenye mafu-
ta.[i] **17** Naye atampasua kwe-
nye mabawa yake. Hatamga-
wanya.[j] Kisha kuhani atamfu-
kiza kwenye madhabahu juu ya
kuni zilizo katika moto. Ni to-
leo la kuteketezwa,[k] toleo lina-
lotolewa kwa njia ya moto lili-
lo na harufu ya kumtuliza Ye-
hova.[l]

2 "'Sasa ikiwa nafsi fulani
itamtolea Yehova toleo la
nafaka,[m] toleo lake litakuwa
la unga laini;[n] naye atamimi-
na mafuta juu yake na kutia
ubani juu yake. **2** Naye atau-
leta kwa wana wa Haruni, ma-
kuhani, naye kuhani atachu-
kua kipimo cha mkono mmo-
ja wa unga huo laini na mafu-
ta yake pamoja na ubani wake
wote; naye ataufukiza uwe ku-
mbukumbu[a] lake kwenye ma-
dhabahu, kama toleo linalotolewa kwa njia ya moto lililo na harufu ya kumtuliza Yehova. **3** Na kilichobaki kutokana na lile toleo la nafaka ni cha Haruni na wanawe,[b] kama kitu kitakatifu[c] zaidi kutoka katika matoleo ya Yehova yanayotolewa kwa njia ya moto.

4 "'Na ikiwa utatoa toleo la nafaka la kitu kilichookwa jikoni, kinapaswa kuwa cha unga laini, keki za mviringo[d] zilizotiwa mafuta zisizo na chachu, au mkate mwembamba uliotiwa mafuta[e] usio na chachu.[f]

5 "'Na ikiwa toleo lako ni toleo la nafaka kutoka katika kiokeo,[g] litakuwa la unga laini uliotiwa mafuta, usio na chachu. **6** Litavunjwa vipande-vipande, nawe utamimina mafuta juu yake.[h] Ni toleo la nafaka.

7 "'Na ikiwa toleo lako ni toleo la nafaka kutoka katika sufuria ya kukaangia, litafanywa kwa unga laini pamoja na mafuta. **8** Nawe utaleta kwa Yehova toleo hilo la nafaka lililofanywa kwa vitu hivyo; nalo litatolewa kwa kuhani naye atalileta karibu na madhabahu. **9** Naye kuhani atachukua sehemu ya toleo hilo la nafaka kuwa kumbukumbu[i] lake na kuifukiza kwenye madhabahu, kuwa toleo linalotolewa kwa njia ya moto lililo na harufu ya kumtuliza Yehova.[j] **10** Na kilichobaki kutoka katika toleo hilo la nafaka ni cha Haruni na wanawe, kama kitu kitakatifu zaidi cha matoleo ya Yehova yanayotolewa kwa njia ya moto.[k]

11 "'Hakuna toleo lolote la nafaka ambalo mtamtolea Yehova

SURA 1
a Law 9:13
1Fa 18:23
b Law 9:14
c Kut 29:17
d Kut 29:18
e Kut 29:41
Law 1:9
f Lu 2:24
g Law 5:7
Law 12:8
h Law 5:8
i Kut 27:3
Law 4:12
Law 6:10
j Mwa 15:10
k Mwa 8:20
Kut 29:18
l Law 6:21
Hes 28:8

SURA 2
m Law 6:14
Law 9:17
Hes 15:4
n Kut 29:2
Hes 7:13

Safu ya 2
a Law 6:15
Hes 5:26
b Law 7:9
c Law 10:12
Hes 18:9
d Kut 29:23
Law 8:26
e Kut 29:2
Law 7:10
Hes 6:15
f Hes 6:19
1Ko 5:7
g Law 6:21
Law 7:9
1Nya 23:29
h Hes 28:9
i Law 2:2
Law 5:12
j Kut 29:41
Hes 28:8
k Hes 18:9
Ebr 13:10

litakalofanywa kuwa kitu kilichotiwa chachu,[a] kwa sababu hamtafukiza unga wowote uliokandwa wenye chachu wala asali yoyote, kuwa toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto.

12 "'Likiwa ni toleo la mazao ya kwanza,[b] mtamtolea Yehova vitu hivyo, navyo visiletwe juu ya madhabahu viwe harufu ya kutuliza.

13 "'Na kila toleo kati ya toleo lako la nafaka utalikoleza kwa chumvi;[c] wala usikubali chumvi ya agano[d] la Mungu wako ikosekane kwenye toleo lako la nafaka. Pamoja na kila toleo lako utatoa chumvi.

14 "'Na ikiwa utamtolea Yehova toleo la nafaka la matunda ya kwanza yaliyoiva, utatoa masuke mabichi yaliyookwa kwa moto, chenga-chenga za nafaka mpya, kuwa toleo la matunda yako ya kwanza yaliyoiva.[e] **15** Nawe utatia mafuta juu yake na kuweka ubani juu yake. Ni toleo la nafaka.[f] **16** Naye kuhani atafukiza kumbukumbu[g] lake, yaani, sehemu ya chenga-chenga zake na mafuta, pamoja na ubani wake wote, kuwa toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto.

3 "'Na ikiwa toleo lake ni dhabihu ya ushirika,[h] ikiwa analitoa kutoka kati ya mifugo, wa kiume au wa kike, atamtoa yule asiye na kasoro[i] mbele za Yehova. **2** Naye atauweka mkono wake juu ya kichwa[j] cha toleo lake, nalo litachinjwa kwenye mwingilio wa hema la mkutano; nao wana wa Haruni, makuhani, watainyunyiza damu yake kwenye madhabahu kuizunguka pande zote. **3** Naye atatoa sehemu ya dhabihu hiyo ya ushirika kuwa toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto, yaani, mafuta[a] yanayofunika matumbo, naam, mafuta yote yaliyo juu ya matumbo,[b] **4** na zile figo mbili[c] na mafuta yaliyo juu yake, sawa na yale yaliyo juu ya viuno. Na kile kipasho kilicho juu ya ini, atakiondoa pamoja na figo. **5** Nao wana wa Haruni[d] wataifukiza[e] kwenye madhabahu, juu ya toleo la kuteketezwa lililo juu ya kuni[f] zilizo katika moto, kuwa toleo linalotolewa kwa njia ya moto lililo na harufu ya kumtuliza[g] Yehova.

6 "'Na ikiwa toleo lake linatoka kati ya kundi kwa ajili ya dhabihu ya ushirika kwa Yehova, wa kiume au wa kike, atamtoa yule asiye na kasoro.[h] **7** Ikiwa anamtoa kondoodume mchanga awe toleo lake, basi atamtoa mbele za Yehova.[i] **8** Naye atauweka mkono wake juu ya kichwa[j] cha toleo lake, nalo litachinjwa[k] mbele ya hema la mkutano; nao wana wa Haruni watainyunyiza damu yake kwenye madhabahu kuizunguka pande zote. **9** Na kutoka katika dhabihu ya ushirika atatoa mafuta yake kuwa toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto.[l] Mkia wote wenye mafuta[m] ndio atakaoutoa karibu na uti wa mgongo, na mafuta yanayofunika matumbo, ndiyo, mafuta yote yaliyo juu ya matumbo,[n] **10** na zile figo mbili na yale mafuta yaliyo juu yake, yale yaliyo juu ya viuno. Na kile kipasho[o] kilicho juu ya ini, atakiondoa pamoja na figo. **11** Na kuhani atavifukiza[p] kwenye

SURA 2
a Kut 12:19; Law 6:17; Mt 16:12; 1Ko 5:7; Ga 5:9
b Kut 23:19; Hes 15:20; 2Nya 31:5; Met 3:9; 1Ko 15:20; Ufu 14:4
c Eze 43:24
d Hes 18:19; 2Nya 13:5
e Kut 23:16; Kut 34:22; Hes 28:26
f Yer 17:26; Yer 41:5
g Kut 29:25; Law 5:12

SURA 3
h Law 22:21
i Hes 6:14
j Kut 29:10; Law 8:18

Safu ya 2
a Kut 29:13; Law 7:23; Law 7:30; 1Fa 8:64; Eze 44:15
b Law 1:13
c Law 3:15; Law 7:4; Law 8:16
d Hes 3:2; Mal 2:4
e Law 1:9; Law 7:31; Law 9:10
f Law 6:12
g Law 1:17; Law 4:31; Efe 5:2
h Kut 12:5; Hes 6:14; 2Ko 5:21; Ebr 7:26; 1Pe 1:19
i Ebr 9:14
j Law 4:4
k Law 4:15
l 2Nya 7:7
m Kut 29:22; Law 9:19
n Law 3:3
o Law 4:9; Law 9:10
p Law 3:5; Law 4:31

madhabahu kama chakula,[a] toleo linalotolewa kwa Yehova
kwa njia ya moto.
12 "'Na ikiwa toleo lake ni
mbuzi,[b] basi atamtoa mbele
za Yehova. **13** Naye atauwe-
ka mkono wake juu ya kichwa
chake,[c] naye atachinjwa[d] mbe-
le ya hema la mkutano; nao
wana wa Haruni watainyunyi-
za damu yake kwenye madha-
bahu kuizunguka pande zote.
14 Na kutokana naye atatoa to-
leo lake, kuwa toleo linalo-
tolewa kwa Yehova kwa njia
ya moto, mafuta yanayofuni-
ka matumbo, naam, mafuta
yote yaliyo juu ya matumbo,[e]
15 na zile figo mbili na mafu-
ta yaliyo juu yake, yale yali-
yo juu ya viuno. Na kile kipasho
kilicho juu ya ini, atakiondoa
pamoja na hizo figo. **16** Naye
kuhani atavifukiza juu ya ma-
dhabahu kama chakula, toleo
linalotolewa kwa njia ya moto
kuwa harufu ya kutuliza. Ma-
futa yote ni ya Yehova.[f]
17 "'Ni sheria mpaka wakati
usio na kipimo kwa ajili ya vi-
zazi vyenu, katika makao yenu
yote: msile mafuta yoyote wala
damu[g] yoyote.'"

4 Na Yehova akaendelea ku-
sema na Musa, na kumwa-
mbia: **2** "Sema na wana wa
Israeli, uwaambie, 'Ikiwa nafsi
itatenda dhambi[h] bila kukusu-
dia[i] katika yoyote kati ya ma-
mbo ambayo Yehova ameamuru
yasifanywe, na kwa kweli afa-
nye moja kati ya mambo hayo:
3 "'Kuhani, aliyetiwa mafu-
ta,[j] akitenda dhambi[k] na kuleta
hatia juu ya watu, basi, kwa aji-
li ya dhambi yake ambayo ame-
tenda,[l] atamtolea Yehova ng'o-
mbe-dume mchanga ambaye
hana kasoro, kuwa toleo la dha-
mbi. **4** Naye atamleta ng'o-
mbe huyo kwenye mwingilio
wa hema la mkutano[a] mbele
za Yehova na kuuweka mkono
wake juu ya kichwa cha ng'o-
mbe huyo,[b] naye atamchinja
ng'ombe huyo mbele za Yeho-
va. **5** Naye kuhani, aliyetiwa
mafuta,[c] atachukua sehemu ya
damu ya ng'ombe huyo na kui-
leta ndani ya hema la mkutano;
6 naye kuhani atachovya kido-
le[d] chake ndani ya damu hiyo
na kutapanya sehemu ya damu
hiyo mara saba[e] mbele za Yeho-
va mbele ya pazia la mahali pa-
takatifu. **7** Naye kuhani ata-
tia sehemu ya damu hiyo juu ya
pembe[f] za madhabahu ya uvu-
mba uliotiwa manukato mbele
za Yehova, iliyo ndani ya hema
la mkutano, na damu yote ili-
yobaki ya ng'ombe huyo atai-
mimina kwenye msingi[g] wa ma-
dhabahu ya toleo la kuketete-
zwa, iliyo kwenye mwingilio wa
hema la mkutano.
8 "'Na mafuta yote ya ng'o-
mbe huyo wa toleo la dha-
mbi atayaondoa kutoka kwa-
ke, mafuta yanayofunika matu-
mbo, ndiyo, mafuta yote yali-
yo juu ya matumbo,[h] **9** na zile
figo mbili na mafuta yaliyo juu
yake, yale yaliyo juu ya viuno.
Nacho kipasho kilicho juu ya
ini, atakiondoa pamoja na figo.[i]
10 Kitakuwa kama kile kili-
choondolewa kutoka kwa yule
ng'ombe-dume wa dhabihu ya
ushirika.[j] Naye kuhani atavifu-
kiza kwenye madhabahu ya to-
leo la kuketetezwa.[k]
11 "'Lakini ngozi ya ng'o-
mbe-dume huyo na nyama yake
yote pamoja na kichwa cha-
ke na miguu yake na matumbo
yake na mavi yake,[l] **12** ata-
mtoa ng'ombe mzima mpaka

SURA 3
a Law 21:6
b Law 9:3
Law 22:19
c Kut 29:10
Law 3:2
d Kut 29:11
Law 3:8
Law 14:13
e Law 3:3
Law 3:9
Law 4:26
Zb 20:3
f Law 7:23
1Sa 2:16
g Mwa 9:4
Law 17:10
Law 17:13
Kum 12:23
Eze 44:7
Mdo 15:20

SURA 4
h Mwa 46:26
i Law 5:17
Hes 15:28
Zb 119:67
Ga 6:1
Yak 2:10
j Law 8:12
Law 21:10
Lu 4:18
Ebr 1:9
k Hes 12:1
Ebr 4:15
Ebr 7:26
l Ebr 5:3
Ebr 7:27

Safu ya 2
a Law 1:3
Law 6:25
b Kut 29:10
Law 1:4
c Kut 29:29
Kut 30:30
d Law 8:15
Law 16:19
e Law 16:14
f Kut 30:10
g Law 5:9
h Law 4:19
Law 4:26
i Law 3:4
Law 9:10
j Law 3:3
k Law 4:26
Zb 20:3
Ebr 10:8
l Kut 29:14
Hes 19:5

nje ya kambi[a] katika mahali safi ambapo yale majivu yenye mafuta[b] humwagwa, naye atamteketeza juu ya kuni kwenye moto.[c] Mahali ambapo majivu yenye mafuta humwagwa, anapaswa kuteketezwa hapo.

13 "'Na kusanyiko lote la Israeli likifanya kosa[d] na jambo hilo limefichwa machoni pa kutaniko ya kwamba wamefanya moja kati ya mambo yote ambayo Yehova ameamuru yasifanywe na kwa hiyo wamekuwa na hatia,[e] **14** nayo dhambi ambayo wamefanya kinyume cha moja kati ya mambo hayo imejulikana,[f] basi kutaniko litatoa ng'ombe-dume mchanga kwa ajili ya toleo la dhambi na kumleta mbele ya hema la mkutano. **15** Na wanaume wazee wa kusanyiko wataweka mikono yao juu ya kichwa cha ng'ombe[g] huyo mbele za Yehova, na ng'ombe huyo atachinjwa mbele za Yehova.

16 "'Kisha kuhani, aliyetiwa mafuta,[h] ataleta sehemu ya damu ya ng'ombe-dume huyo ndani ya hema la mkutano.[i] **17** Naye kuhani atachovya kidole chake katika sehemu ya damu hiyo na kuitapanya mara saba mbele za Yehova mbele ya pazia.[j] **18** Naye atatia sehemu ya damu hiyo juu ya pembe za madhabahu[k] iliyo mbele za Yehova, ambayo imo ndani ya hema la mkutano; na damu yote inayobaki ataimimina kwenye msingi wa madhabahu ya toleo la kuteketezwa,[l] iliyo kwenye mwingilio wa hema la mkutano. **19** Naye atachukua mafuta yake yote, na kuyafukiza kwenye madhabahu.[m] **20** Naye atamfanya huyo ng'ombe-dume kama alivyomfanya yule ng'ombe mwingine wa toleo la dhambi. Hivyo ndivyo atakavyomfanya; naye kuhani atafanya upatanisho[a] kwa ajili yao, ndipo watasamehewa. **21** Naye atamtoa huyo ng'ombe mpaka nje ya kambi na kumteketeza, kama alivyomteketeza ng'ombe-dume wa kwanza.[b] Ni toleo la dhambi kwa ajili ya kutaniko.[c]

22 "'Mkuu[d] anapotenda dhambi naye afanye bila kukusudia moja kati ya mambo yote ambayo Yehova Mungu wake ameamuru yasifanywe,[e] na kwa hiyo amekuwa na hatia, **23** au amejulishwa dhambi yake ambayo amefanya kinyume cha amri,[f] basi atamleta mwana-mbuzi dume[g] ambaye hana kasoro, awe toleo lake. **24** Naye atauweka mkono wake juu ya kichwa[h] cha mwana-mbuzi huyo na kumchinja katika mahali ambapo toleo la kuteketezwa huchinjiwa kwa ukawaida mbele za Yehova.[i] Hilo ni toleo la dhambi.[j] **25** Naye kuhani atachukua sehemu ya damu ya toleo la dhambi kwa kidole chake na kuitia juu ya pembe[k] za madhabahu hiyo ya toleo la kuteketezwa, naye ataimimina damu yake inayobaki kwenye msingi wa madhabahu ya toleo la kuteketezwa. **26** Naye atayafukiza mafuta yake yote kwenye madhabahu kama yale mafuta ya dhabihu ya ushirika;[l] naye kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake kwa ajili ya dhambi zake,[m] naye atasamehewa.

27 "'Na ikiwa nafsi yoyote kati ya watu wa nchi itatenda dhambi bila kukusudia kwa kufanya moja kati ya mambo ambayo Yehova anaamu-

SURA 4

a Hes 5:3
Ebr 13:11
b Law 6:11
c Law 8:17
d Yos 7:11
Met 14:34
e Kut 32:30
Hes 15:24
f Mhu 12:14
1Ti 5:24
g Kut 29:10
Law 1:4
Law 3:2
Law 16:21
Mt 8:17
Ebr 9:28
1Pe 2:24
h Kut 40:15
i Law 4:5
j Kut 26:31
Kut 40:21
Ebr 10:20
k Kut 30:1
Kut 30:6
l Kut 27:1
Kut 40:6
Law 4:7
m Law 3:16

Safu ya 2

a Kut 32:30
Law 12:8
Law 16:17
Hes 15:25
Efe 1:7
1Ti 2:5
Ebr 2:17
b Law 4:12
c Law 16:15
Mt 20:28
Yoh 1:29
1Yo 2:2
d Kut 18:21
Hes 16:2
Hes 34:18
Yos 22:14
2Sa 24:10
e Law 5:4
Law 5:17
Law 6:2
f 2Sa 12:13
g Law 23:19
Hes 15:24
Hes 28:15
Hes 29:5
h Law 1:4
Law 4:4
Met 28:13
Isa 53:6
i Law 1:11
Law 3:2
Law 6:25
Law 7:2
j Law 4:3
k Law 8:15
Law 9:9
Law 16:18
Ebr 9:22
l Law 3:5
m Kut 32:30
Hes 15:28

ru yasifanywe nayo iwe na hatia,[a] **28** au amejulishwa dhambi yake ambayo ametenda, basi atamtoa mwana-mbuzi jike[b] ambaye hana kasoro, awe toleo lake kwa ajili ya dhambi ambayo amefanya. **29** Naye ataweka mkono wake juu ya kichwa[c] cha toleo la dhambi na kulichinja toleo la dhambi katika mahali pale pale pa toleo la kuteketezwa.[d] **30** Naye kuhani atachukua sehemu ya damu yake kwa kidole chake na kuitia juu ya pembe[e] za madhabahu ya toleo la kuteketezwa, naye ataimimina damu yake yote inayobaki kwenye msingi wa madhabahu.[f] **31** Naye atayaondoa mafuta yake yote,[g] kama mafuta yalivyoondolewa kwenye dhabihu ya ushirika;[h] naye kuhani atayafukiza kwenye madhabahu yawe harufu ya kumtuliza Yehova;[i] naye kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake, naye atasamehewa.[j]

32 "'Lakini ikiwa atamleta mwana-kondoo[k] awe toleo lake la dhambi, atamleta mwana-kondoo jike ambaye hana kasoro.[l] **33** Naye atauweka mkono wake juu ya kichwa cha toleo la dhambi na kumchinja awe toleo la dhambi katika mahali pale ambapo toleo la kuteketezwa huchinjiwa.[m] **34** Naye kuhani atachukua sehemu ya damu hiyo ya toleo la dhambi kwa kidole chake na kuitia juu ya pembe za madhabahu ya toleo la kuteketezwa,[n] naye ataimimina damu yake yote inayobaki kwenye msingi wa madhabahu. **35** Naye atayaondoa mafuta yake yote kama mafuta ya mwana-kondoo dume wa dhabihu ya ushirika yanavyoondolewa kwa ukawaida, naye kuhani atayafukiza kwenye madhabahu juu ya matoleo ya Yehova yanayotolewa kwa njia ya moto;[a] naye kuhani atafanya upatanisho[b] kwa ajili yake kwa ajili ya dhambi ambayo amefanya, naye atasamehewa.[c]

5 "'Ikiwa nafsi[d] inatenda dhambi kwa kuwa amesikia laana[e] ya hadharani naye ni shahidi au ameiona au amepata kujua juu yake, asipotoa habari,[f] ndipo atakapojibu kwa sababu ya kosa lake.

2 "'Au nafsi inapogusa kitu kisicho safi, iwe ni mzoga wa mnyama-mwitu asiye safi au mzoga wa mnyama wa kufugwa asiye safi au mzoga wa kiumbe kinachozaana kwa wingi kisicho safi,[g] ingawa ulikuwa umefichwa machoni pake,[h] bado yeye si safi naye amekuwa na hatia.[i] **3** Au ikiwa anagusa uchafu wa mwanadamu kuhusiana na uchafu[j] wowote wake ambao huenda ukamfanya asiwe safi, ingawa ulikuwa umefichwa machoni pake, na hata hivyo yeye mwenyewe amepata kujua, basi amekuwa na hatia.

4 "'Au ikiwa nafsi inaapa kiasi cha kusema kwa midomo yake bila kufikiri[k] kwamba itende uovu[l] au kufanya mema kuhusiana na jambo lolote ambalo huenda mtu huyo akasema bila kufikiri katika ahadi yenye kiapo,[m] ingawa lilikuwa limefichwa machoni pake, na hata hivyo yeye mwenyewe amepata kulijua, basi amekuwa na hatia kuhusiana na moja kati ya mambo hayo.

5 "'Na itakuwa kwamba ikiwa anakuwa na hatia kwa sababu ya moja kati ya mambo

SURA 4

a Kut 12:49; Hes 5:6; Hes 15:29
b Law 5:6
c Law 1:4; Law 3:2; Law 4:4; Law 16:21; Met 28:13; Isa 53:6; Mt 8:17; 1Pe 2:24
d Law 1:11; Law 6:25
e Law 4:25
f Law 8:15; Law 9:9; Ebr 9:22
g Law 3:16; Law 4:8
h Law 3:3
i Kut 29:18; Law 1:9; Law 3:5; Law 8:21; Ezr 6:10
j Law 4:26; Ho 14:2
k Isa 53:7; Yoh 1:29; Ebr 9:14; 1Pe 1:19
l Law 3:6; Ebr 7:26; Ebr 9:14; 1Pe 2:22
m Law 1:11; Law 4:4
n Law 4:25; Law 16:18

Safu ya 2

a Kut 29:13; Law 3:3; Law 6:12; Law 9:10
b Law 1:4; Law 4:26; Law 4:31; Law 6:7; Law 16:30; Hes 15:28; Kol 1:14; 1Yo 2:2
c 1Yo 1:7

SURA 5

d Mwa 2:7; Mwa 46:26; Eze 18:4
e Met 29:24
f Mwa 37:2; 1Sa 2:24; Est 6:2; Met 29:24; 1Ko 1:11; 1Ko 5:1
g Law 11:24; Law 17:15; Law 21:1; Hes 19:11; Kum 14:8
h Zb 19:12
i Law 4:13
j Law 12:2; Law 13:3; Law 15:3; Hes 19:11
k Yak 3:8; 1Pe 3:10
l Mal 3:5
m Amu 21:7; 1Sa 14:24; Mt 5:33; Mk 6:23

hayo, ndipo atakapoungama[a] jinsi ambavyo ametenda dhambi.
6 Naye ataleta toleo lake la hatia[b] mbele za Yehova kwa ajili
ya dhambi yake ambayo ametenda, yaani, wa kike kutoka ka-
tika kundi, mwana-kondoo jike
au mwana-mbuzi jike,[c] kwa ajili
ya toleo la dhambi; naye kuha-
ni atamfanyia upatanisho kwa
ajili ya dhambi yake.[d]
7 "'Hata hivyo, ikiwa hana
uwezo wa kutoa kondoo,[e] basi
atamletea Yehova njiwa-tetere[f]
wawili au hua wawili wachanga
wawe toleo lake la hatia[g] kwa
ajili ya dhambi ambayo ameten-
da, mmoja kwa ajili ya toleo la
dhambi na mmoja kwa ajili ya
toleo la kuteketezwa. **8** Naye
atawaleta kwa kuhani, amba-
ye kwanza atamtoa yule wa to-
leo la dhambi na kukongonyoa[h]
kichwa chake upande wa mbe-
le wa shingo yake, lakini asiki-
kate kabisa. **9** Naye atatapa-
nya sehemu ya damu ya toleo
la dhambi kando ya madhaba-
hu, lakini damu inayobaki ita-
achwa itiririke kwenye msingi
wa madhabahu.[i] Hilo ni toleo la
dhambi. **10** Na yule mwingi-
ne atamtoa kuwa toleo la ku-
teketezwa kulingana na utara-
tibu wa kawaida;[j] naye kuhani
atafanya upatanisho[k] kwa aji-
li yake kwa sababu ya dhambi
yake ambayo ametenda, naye
atasamehewa.[l]
11 "'Sasa ikiwa hana uwezo[m]
wa kutoa njiwa-tetere wawili
au hua wawili wachanga, basi
ataleta sehemu ya kumi ya efa[n]
ya unga laini kwa ajili ya to-
leo la dhambi, uwe toleo lake la
dhambi. Naye hatatia mafuta[o]
juu yake wala hataweka uba-
ni juu yake, kwa maana ni to-
leo la dhambi.[p] **12** Naye atau-

SURA 5

a Law 26:40 Hes 5:7 Yos 7:19 Ezr 10:11 Zb 32:5 Met 28:13 1Yo 1:9
b Law 7:1 Law 14:12 Law 19:21 Hes 6:12
c Law 4:28
d Law 4:20 Yoh 1:29 1Ti 2:5 Ebr 9:14 1Yo 4:10
e Law 12:8 Law 14:21 2Ko 8:12 Yak 2:5
f Law 1:14 Law 15:14
g Law 14:22 Lu 2:24
h Law 1:15
i Law 1:5 Law 7:2 Ebr 9:22
j Law 1:17
k Law 6:7 Ebr 2:17 1Yo 2:2
l Kut 34:9
m 2Ko 8:12
n Kut 16:36
o Hes 5:15
p Law 5:6 Met 28:13 2Ko 5:21

Safu ya 2

a Law 6:15 Hes 5:26
b Law 4:35
c Law 4:3
d Law 4:26
e Law 2:10 Law 7:6 1Sa 2:28 1Ko 9:13
f Law 10:18 Law 22:14 Hes 18:9
g Law 6:6
h Kut 30:13 Law 27:25
i Law 6:5 Law 22:14 Law 27:13 Hes 5:7
j Kut 32:30 Law 12:8 Hes 15:25 Ebr 2:17 1Yo 2:2
k Kut 34:9 Law 4:20 Law 6:7 Law 19:22
l Zb 19:12 Lu 12:48 Ebr 5:2
m Law 5:2 1Ti 5:24

leta kwa kuhani, naye kuhani
atachukua kipimo cha mkono
mmoja uwe kumbukumbu[a] lake
naye ataufukiza kwenye ma-
dhabahu juu ya toleo la Ye-
hova linalotolewa kwa njia ya
moto.[b] Hilo ni toleo la dhambi.[c]
13 Naye kuhani atafanya upa-
tanisho[d] kwa ajili yake kwa sa-
babu ya dhambi yake ambayo
ametenda, yoyote kati ya dha-
mbi hizo, naye atasamehewa;
nao utakuwa wa kuhani[e] sawa
na toleo la nafaka.'"
14 Na Yehova akaendelea
kusema na Musa, na kumwa-
mbia: **15** "Ikiwa nafsi inajien-
desha kwa njia isiyo ya uami-
nifu kwa kutenda dhambi bila
kukusudia juu ya mambo mata-
katifu ya Yehova,[f] basi atamto-
lea Yehova kondoo-dume amba-
ye hana kasoro kutoka kati-
ka kundi, awe toleo lake la ha-
tia,[g] kulingana na ile thamani
iliyokadiriwa ya shekeli za fe-
dha,[h] kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, kuwa to-
leo la hatia. **16** Naye atali-
pa kwa ajili ya dhambi amba-
yo amepatendea mahali pata-
katifu naye ataongeza juu yake
sehemu yake ya tano,[i] naye ata-
mpa kuhani, ili kuhani afanye
upatanisho[j] kwa ajili yake kwa
kutumia yule kondoo-dume wa
toleo la hatia, naye atasame-
hewa.[k]
17 "Na ikiwa nafsi inatenda
dhambi kwa kuwa anafanya
moja kati ya mambo ambayo
Yehova anaamuru yasifanywe,
ingawa hakujua,[l] hata hivyo
amekuwa na hatia na lazima
atajibu kwa sababu ya kosa
lake.[m] **18** Naye atamleta ko-
ndoo-dume ambaye hana kaso-
ro kutoka katika kundi kuli-
ngana na thamani iliyokadiri-

wa, kwa ajili ya toleo la ha-
tia,[a] kwa kuhani; naye kuhani
atafanya upatanisho[b] kwa aji-
li yake kwa sababu ya kosa ali-
lofanya bila kukusudia, ingawa
yeye mwenyewe hakujua, naye
atasamehewa.[c] **19** Hilo ni toleo
la hatia.[d] Hakika amekuwa
na hatia dhidi ya Yehova."

6 Na Yehova akaendelea ku-
sema na Musa, na kumwa-
mbia: **2** "Ikiwa nafsi inatenda
dhambi, kwa kujiendesha kwa
njia isiyo ya uaminifu kwa Ye-
hova[e] naye amdanganye[f] mwe-
nzake juu ya kitu fulani alicho
nacho au arbuni iliyo mkono-
ni mwake[g] au kumnyang'anya,
au ampunje mwenzake,[h] **3** au
apate kitu kilichopotea[i] naye
adanganye kuhusu kitu hicho
na kuapa kwa uwongo[j] juu ya
jambo lolote kati ya mambo
yote ambayo huenda mtu huyo
akafanya na kutenda dhambi
kutokana nayo; **4** basi itaku-
wa kwamba akitenda dhambi
na kuwa na hatia,[k] lazima ata-
rudisha kile kitu alichopata
kwa unyang'anyi au alicho-
pata kwa upokonyaji amba-
cho amechukua kwa kupunja
au kitu alicho nacho amba-
cho alipewa au kitu kilichopo-
tea ambacho amekipata, **5** au
kitu chochote ambacho huenda
akaapa juu yake kwa uwongo,
naye atatoa malipo[l] kwa ajili
yake kwa kiwango chake kami-
li, naye ataongezea juu yake se-
hemu yake ya tano. Siku amba-
yo hatia yake itahakikishwa
atampa mwenyewe kitu hicho.
6 Naye atamletea Yehova toleo
la hatia, kondoo-dume amba-
ye hana kasoro[m] kutoka katika
kundi kulingana na thamani
iliyokadiriwa, kwa ajili ya toleo
la hatia,[n] kwa kuhani. **7** Naye

SURA 5
a Law 5:7
Law 6:6
b Law 1:4
c Isa 53:12
d Ezr 10:2
Zb 51:3

SURA 6
e Law 5:15
Hes 5:6
Zb 51:4
f Law 19:11
g Kut 22:7
h Ayu 24:2
Mik 2:2
Mdo 13:10
i Kum 22:1
j Kut 22:11
Law 19:12
Yer 7:9
Mal 3:5
Efe 4:25
Kol 3:9
1Ti 1:10
k Law 4:13
l Law 5:16
Hes 5:7
1Sa 12:3
m Law 5:15
Isa 53:10
Ebr 9:14
n Law 7:1

Safu ya 2
a Law 4:20
Law 5:10
Law 5:18
1Yo 1:7
1Yo 2:2
b Kut 29:42
Hes 28:3
Ebr 10:11
c Kut 28:39
Law 16:32
Ezr 3:10
Eze 44:17
d Kut 28:42
Kut 39:28
e Kut 27:3
Law 1:16
Law 4:12
f Law 16:23
Eze 44:19
g Law 4:12
Law 16:27
Hes 19:9
Ebr 13:12
h Law 1:7
Law 3:5
Ne 13:31
i Law 3:5
Law 3:16
Hes 18:17
j Hes 16:46
k Law 2:1
Hes 15:4

kuhani atafanya upatanisho[a]
kwa ajili yake mbele za Yehova,
naye atasamehewa lolote amba-
lo huenda akafanya kati ya ma-
mbo yote hayo, nalo limfanye
awe na hatia."

8 Na Yehova akaendelea ku-
sema na Musa, na kumwambia:
9 "Mwamuru Haruni na wana-
we, na kusema, 'Hii ndiyo she-
ria ya toleo la kuteketezwa:[b]
Toleo la kuteketezwa litakuwa
kwenye jiko juu ya madhaba-
hu usiku kucha mpaka asubuhi,
nao moto wa madhabahu uta-
washwa ndani yake. **10** Naye
kuhani atajivika nguo yake ra-
smi ya kitani,[c] naye atavaa ile
surali[d] ya kitani mwilini mwa-
ke. Kisha atayachukua yale
majivu yenye mafuta[e] ya to-
leo la kuteketezwa ambayo hu-
teketezwa kwa moto kwa uka-
waida juu ya madhabahu, naye
atayaweka kando ya madhaba-
hu. **11** Naye atayavua mavazi[f]
yake na kuvaa mavazi mengi-
ne, naye atayachukua yale maji-
vu yenye mafuta mpaka ma-
hali safi nje ya kambi.[g] **12** Na
huo moto kwenye madhabahu
utaendelea kuwaka juu yake.
Usizimike. Naye kuhani atate-
keteza kuni[h] juu yake asubu-
hi baada ya asubuhi na kuweka
kwa utaratibu toleo la kuteke-
tezwa juu yake, naye atafukiza
vile vipande vyenye mafuta vya
dhabihu ya ushirika juu yake.[i]
13 Moto[j] utawaka daima kwe-
nye madhabahu. Usizimike.

14 "'Hii ndiyo sheria ya to-
leo la nafaka:[k] Ninyi wana wa
Haruni, litoeni mbele za Yehova
mbele ya madhabahu. **15** Na
mmoja wao atachukua kipimo
cha mkono mmoja wa huo unga
laini wa toleo la nafaka na se-
hemu ya mafuta yake na ubani

wote ulio juu ya toleo hilo la nafaka, naye ataufukiza kwenye madhabahu uwe harufu ya kutuliza ya kumbukumbu[a] lake kwa Yehova. **16** Na ule unaobaki, Haruni na wanawe watawala.[b] Utaliwa kama keki zisizo na chachu[c] katika mahali patakatifu. Wataula kwenye ua wa hema la mkutano. **17** Hautaokwa pamoja na kitu chochote kilichotiwa chachu.[d] Nimeutoa uwe fungu lao kutoka katika matoleo yangu yanayotolewa kwa njia ya moto.[e] Ni kitu kitakatifu zaidi,[f] kama lile toleo la dhambi na kama lile toleo la hatia. **18** Kila mwanamume[g] kati ya wana wa Haruni ataula. Ni posho kutoka katika matoleo ya Yehova yanayotolewa kwa njia ya moto, mpaka wakati usio na kipimo[h] katika vizazi vyenu vyote. Chochote kitakachoyagusa kitakuwa kitakatifu.'"

19 Naye Yehova akaendelea kusema na Musa, na kumwambia: **20** "Hili ndilo toleo[i] la Haruni na wanawe ambalo watamtolea Yehova siku ya kutiwa mafuta kwake:[j] sehemu ya kumi ya efa[k] ya unga laini uwe toleo la nafaka[l] daima, nusu yake asubuhi na nusu yake jioni. **21** Utatolewa pamoja na mafuta kwenye kiokeo.[m] Utauleta ukiwa umechanganywa vizuri. Utatoa vitumbua vya toleo la nafaka vipande-vipande viwe harufu ya kumtuliza Yehova. **22** Na kuhani, aliyetiwa mafuta badala yake kati ya wanawe,[n] atatoa toleo hilo. Ni sharti mpaka wakati usio na kipimo: Hilo toleo zima litafukizwa[o] kwa Yehova. **23** Na kila toleo la nafaka la kuhani[p] litakuwa toleo zima. Halitaliwa."

SURA 6

a Law 2:2
Law 2:9
Law 5:12
b Law 2:3
Law 5:13
Eze 44:29
1Ko 9:13
c Law 10:12
d Law 2:11
Mt 16:12
1Pe 2:22
e Hes 18:9
f Law 2:3
Law 2:10
g Hes 18:10
h Law 24:9
i Kut 29:2
j Kut 30:30
Zb 133:2
Lu 4:18
Mdo 10:38
Ebr 1:9
Ebr 5:1
Ebr 7:28
Ebr 8:3
k Kut 16:36
Law 5:11
l Kut 29:40
Law 2:1
Law 9:17
Hes 28:5
m Law 2:5
Law 7:9
1Nya 23:29
n Kum 10:6
Ebr 7:23
o Kut 29:41
p Ebr 7:28

Safu ya 2

a Law 4:3
b Law 1:3
Law 1:11
c Law 21:22
Law 22:7
d Law 10:17
Hes 18:9
Eze 44:29
e Law 6:16
f Kut 27:9
Kut 38:9
Kut 40:33
Eze 42:13
g Mt 9:21
Mt 14:36
h 1Pe 1:2
i Ebr 9:10
j Law 11:33
Law 15:12
k Law 6:18
Hes 18:10
l Law 6:25
Law 21:22
m Law 4:5
Law 10:18
Law 16:27
Ebr 13:11

SURA 7

n Law 5:6
Law 6:6
Law 14:12
Law 19:21
Hes 6:12
o Law 6:17
Law 21:22
p Law 1:3
Law 6:25
q Law 5:9
Ebr 9:22
r Law 1:5
Law 3:2
Law 5:9
1Pe 1:2

24 Naye Yehova akazidi kusema na Musa, na kumwambia: **25** "Sema na Haruni na wanawe, na kuwaambia, 'Hii ndiyo sheria ya toleo la dhambi:[a] Katika mahali[b] ambapo toleo la kuteketezwa huchinjiwa kwa ukawaida, toleo la dhambi litachinjwa mbele za Yehova. Ni kitu kitakatifu zaidi.[c] **26** Kuhani ambaye hutoa toleo hilo kwa ajili ya dhambi atalila.[d] Katika mahali patakatifu[e] litaliwa katika ua[f] wa hema la mkutano.

27 "'Chochote ambacho huenda kikagusa nyama yake kitakuwa kitakatifu,[g] na mtu yeyote akitapanya damu yake juu ya vazi,[h] utakioshea katika mahali patakatifu kile ambacho ametapanya damu juu yake.[i] **28** Na chombo cha udongo[j] ambamo huenda likatokosewa ndani yake kitavunjwa. Lakini ikiwa lilitokoswa katika chombo cha shaba, basi kitaparuzwa na kuoshwa kwa maji.

29 "'Kila mwanamume kati ya makuhani atalila.[k] Ni kitu kitakatifu zaidi.[l] **30** Hata hivyo, toleo lolote la dhambi ambalo sehemu ya damu[m] yake itaingizwa katika hema la mkutano ili kufanya upatanisho katika mahali patakatifu, halitaliwa. Litateketezwa kwa moto.

7 "'Nayo hii ndiyo sheria ya toleo la hatia:[n] Ni kitu kitakatifu zaidi.[o] **2** Katika mahali[p] ambapo toleo la kuteketezwa huchinjiwa kwa ukawaida, hapo watachinja toleo la hatia, na damu[q] yake atainyunyiza[r] juu ya madhabahu kuizunguka pande zote. **3** Nayo mafuta yake yote,[s] atatoa ule mkia wenye mafuta na mafuta yana-

s Kut 29:13; Law 3:9; Law 3:17; Law 4:8; Law 8:20.

yofunika matumbo, **4** na zile
figo mbili na mafuta yaliyo juu
yake sawa na yale yaliyo juu
ya viuno. Na kile kipasho kili-
cho juu ya ini, atakiondoa pa-
moja na figo.[a] **5** Naye kuhani
atavifukiza kwenye madhaba-
hu viwe toleo linalotolewa kwa
Yehova kwa njia ya moto.[b] Ni
toleo la hatia. **6** Litaliwa na
kila mwanamume kati ya ma-
kuhani.[c] Katika mahali pataka-
tifu litaliwa. Ni kitu kitakatifu
zaidi.[d] **7** Kama toleo la dha-
mbi lilivyo, ndivyo na toleo la
hatia lilivyo. Kuna sheria moja
kwa matoleo hayo.[e] Litaku-
wa la kuhani ambaye atafanya
upatanisho kwa toleo hilo.

8 "'Naye kuhani anayetoa
toleo la kuteketezwa la mtu ye-
yote, ngozi[f] ya toleo la kuteke-
tezwa ambalo mtu huyo amele-
ta kwa kuhani itakuwa yake.

9 "'Na kila toleo la nafaka
ambalo huenda likaokwa kwe-
nye jiko[g] na kila moja lililota-
yarishwa kwenye sufuria ya ku-
kaangia[h] na kwenye kiokeo[i] ni
la kuhani anayelitoa. Litakuwa
lake.[j] **10** Bali kila toleo lililo-
tiwa mafuta[k] au lililo kavu[l] lita-
kuwa la wana wote wa Haruni,
la mmoja sawa na mwingine.

11 "'Sasa hii ndiyo sheria ya
dhabihu ya ushirika[m] amba-
yo mtu yeyote atamtolea Yeho-
va: **12** Ikiwa anaitoa ili kuo-
nyesha shukrani,[n] basi ataitoa
pamoja na dhabihu ya shukra-
ni ya keki za mviringo zisizo na
chachu ambazo zimetiwa mafu-
ta na mikate myembamba isi-
yo na chachu iliyopakwa mafu-
ta[o] na unga laini uliochan-
ganywa vizuri ukiwa keki za
mviringo zilizotiwa mafuta.
13 Atatoa toleo lake pamoja na
ile dhabihu ya shukrani ya dha-

SURA 7

a Law 3:4
Law 4:9
b Law 1:9
Law 3:16
Law 5:12
c Law 5:13
Law 6:16
Hes 18:9
d Law 2:3
e Law 6:25
Law 14:13
f Kut 29:14
Law 1:6
Hes 19:5
g Law 2:4
h Law 2:7
i Law 2:5
Law 6:21
1Nya 23:29
j Law 2:3
Hes 18:9
1Ko 9:13
k Law 2:4
Law 14:21
l Law 5:11
Hes 5:15
m Law 3:1
Law 7:20
Law 22:21
1Ko 10:16
n Law 22:29
2Nya 29:31
Ne 12:43
Zb 50:14
2Ko 9:11
o Law 2:4
Law 6:16
Hes 6:15

Safu ya 2

a Law 2:11
Law 23:17
b Law 10:14
c Law 6:26
Law 7:35
Hes 18:8
d Law 22:30
e Law 22:21
Hes 30:2
Amu 11:30
1Sa 1:11
Zb 66:13
Met 20:25
Mhu 5:4
Mdo 21:23
f Law 22:23
Kum 12:6
g Law 19:6
h Law 19:7
i Mwa 4:5
j Law 5:17
Law 19:8
Hes 9:13
Eze 4:14
k Law 11:24
Hes 19:15
l Law 15:3
Hes 19:20
m Law 12:4
Law 15:2
n Law 11:24
Kum 14:7
o Law 11:10
Kum 14:10
Eze 4:14

bihu zake za ushirika na kuzi-
ambatanisha na keki za mviri-
ngo za mkate wenye chachu.[a]
14 Na kutoka katika hiyo ata-
toa moja kati ya kila toleo liwe
fungu takatifu kwa Yehova;[b]
nalo litakuwa la kuhani[c] anaye-
nyunyiza damu ya dhabihu za
ushirika. **15** Nayo nyama ya
dhabihu ya shukrani ya dhabi-
hu zake za ushirika italiwa siku
yake ya kutoa toleo. Hataweka akiba yoyote ya nyama hiyo
mpaka asubuhi.[d]

16 "'Na ikiwa dhabihu ya to-
leo lake ni toleo la nadhiri[e]
au la hiari,[f] italiwa siku
atakayoitoa dhabihu yake, na
kesho yake kilichobaki kina-
weza kuliwa. **17** Lakini nya-
ma inayobaki ya dhabihu katika siku ya tatu, itateketezwa
kwa moto.[g] **18** Hata hivyo,
ikiwa nyama yoyote ya dhabi-
hu yake ya ushirika italiwa ka-
tika siku ya tatu, yule anaye-
itoa hatapata kibali.[h] Haitahe-
sabiwa kwake.[i] Itakuwa kitu
kichafu, nayo nafsi ambayo
itakula sehemu yake itajibu
kwa kosa lake.[j] **19** Nayo nya-
ma itakayogusa kitu chochote
kisicho safi[k] isiliwe. Itateketezwa kwa moto. Kuhusu nyama
ile nyingine, kila mtu aliye safi
anaweza kuila nyama hiyo.

20 "'Nayo nafsi inayokula
nyama ya dhabihu ya ushiri-
ka, ambayo ni ya Yehova, wa-
kati ambapo uchafu wake uko
juu yake, nafsi hiyo itakatiliwa
mbali na watu wake.[l] **21** Na
ikiwa nafsi itagusa kitu cho-
chote kisicho safi, uchafu wa
mwanadamu[m] au mnyama asi-
ye safi[n] au kitu chochote che-
nye kuchukiza kisicho safi,[o]
naye ale sehemu ya nyama ya
dhabihu ya ushirika, ambayo ni

ya Yehova, nafsi hiyo itakatiliwa mbali na watu wake.'"

22 Naye Yehova akaendelea kusema na Musa, na kumwambia: **23** "Sema na wana wa Israeli, na kuwaambia, 'Msile mafuta[a] yoyote ya ng'ombe-dume au ya mwana-kondoo dume au ya mbuzi. **24** Sasa mafuta ya mzoga ambao tayari umekufa na mafuta ya mnyama aliyeraruliwa[b] vipande-vipande yanaweza kutumiwa kwa ajili ya kitu kingine chochote kinachoweza kufikiriwa, lakini ninyi msiyale hata kidogo. **25** Kwa maana mtu yeyote anayekula mafuta kutoka kwa mnyama anayemtoa awe toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto, nafsi inayokula itakatiliwa mbali[c] na watu wake.

26 "'Wala msile damu[d] yoyote mahali popote mnapokaa, iwe ni ya ndege au ya mnyama. **27** Nafsi yoyote inayokula damu yoyote, nafsi hiyo itakatiliwa mbali[e] na watu wake.'"

28 Naye Yehova akaendelea kusema na Musa, na kumwambia: **29** "Sema na wana wa Israeli, na kuwaambia, 'Mtu anayemtolea Yehova dhabihu yake ya ushirika atamletea Yehova toleo lake kutoka katika dhabihu yake ya ushirika.[f] **30** Mikono yake italeta yale mafuta[g] yaliyo kwenye kidari yawe toleo la Yehova linalotolewa kwa njia ya moto. Atayaleta pamoja na kidari hicho ili akitikise huku na huku kikiwa toleo la kutikisa[h] mbele za Yehova. **31** Naye kuhani atayafukiza[i] mafuta kwenye madhabahu, lakini kidari kitakuwa cha Haruni na wanawe.[j]

32 "'Nanyi mtampa kuhani mguu wa kuume uwe fungu[k] takatifu kutoka katika dhabihu zenu za ushirika. **33** Kati ya wana wa Haruni, yule atakayeitoa damu ya dhabihu ya ushirika na yale mafuta, ule mguu wa kuume utakuwa fungu lake.[a] **34** Kwa maana kidari cha toleo la kutikisa[b] na mguu wa lile fungu takatifu navichukua kutoka kwa wana wa Israeli kutoka katika dhabihu zao za ushirika, nami nitampa Haruni kuhani na wanawe kutoka kwa wana wa Israeli, kama sharti mpaka wakati usio na kipimo.

35 "'Hili ndilo lililokuwa fungu la kuhani la Haruni na fungu la kuhani la wanawe kutoka katika matoleo ya Yehova yanayotolewa kwa njia ya moto, katika siku ambayo aliwatoa[c] watumikie wakiwa makuhani kwa Yehova, **36** kama vile Yehova alivyokuwa ameamuru wapewe katika siku ya kutiwa mafuta[d] kwao kutoka kati ya wana wa Israeli. Ni kanuni mpaka wakati usio na kipimo katika vizazi vyao.'"[e]

37 Hii ndiyo sheria inayohusu toleo la kuteketezwa,[f] toleo la nafaka[g] na toleo la dhambi[h] na toleo la hatia[i] na dhabihu ya kuweka rasmi[j] na dhabihu ya ushirika,[k] **38** kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa kwenye Mlima Sinai[l] katika siku aliyowaamuru wana wa Israeli wamtolee Yehova matoleo yao katika nyika ya Sinai.[m]

8 Naye Yehova akaendelea kusema na Musa, na kumwambia: **2** "Mchukue Haruni na wanawe pamoja naye[n] na yale mavazi[o] na yale mafuta yanayotumiwa kutia mafuta[p] na yule ng'ombe-dume na toleo la dhambi[q] na wale kondoo-dume wawili na kile

SURA 7

a Law 3:16
Law 3:17
Law 4:8
1Sa 2:16
b Kut 22:31
Law 17:15
c Hes 15:31
d Mwa 9:4
Law 3:17
Law 17:10
Kum 12:16
1Sa 14:33
Eze 33:25
Mdo 15:20
Mdo 15:29
e Law 17:14
f Law 3:1
1Ko 10:18
g Law 3:3
h Kut 29:24
Law 8:27
Law 9:21
Hes 6:20
i Law 3:5
j Law 5:13
Law 6:16
Law 8:29
Hes 18:18
k Kut 29:27
Law 10:14
Hes 6:20

Safu ya 2

a Law 6:26
Kum 18:3
b Kut 29:28
Law 10:14
Hes 18:18
c Kut 28:1
Kut 29:7
Kut 40:13
Hes 18:7
d Kut 40:15
Law 8:12
e Ebr 7:12
f Law 6:9
Amo 5:22
Mk 12:33
Ebr 10:5
Ebr 10:6
g Law 2:1
Law 6:14
h Law 6:25
i Law 5:6
Law 7:1
j Kut 29:1
Law 6:20
k Law 3:1
l Kut 34:27
Law 25:1
m Kut 24:5
Law 1:2

SURA 8

n Kut 28:1
o Kut 28:4
Kut 39:41
p Kut 30:23
Kut 40:15
q Kut 29:1

kikapu cha keki zisizo na chachu,[a] **3** nawe ukutanishe kusanyiko lote[b] kwenye mwingilio wa hema la mkutano."[c]

4 Ndipo Musa akafanya kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru, nalo kusanyiko likakutanika kwenye mwingilio[d] wa hema la mkutano. **5** Sasa Musa akaliambia kusanyiko: "Hili ndilo jambo ambalo Yehova ametoa amri lifanywe."[e] **6** Basi Musa akawaleta karibu Haruni na wanawe na kuwaosha[f] kwa maji.[g] **7** Baada ya hayo akamvika kanzu[h] na kumfunga ukumbuu[i] na kumvika lile koti lisilo na mikono[j] na kumvika efodi[k] na kumfunga kwa mshipi[l] wa ile efodi na kuufunga imara kwa mshipi huo. **8** Kisha akamvika kile kifuko cha kifuani[m] na kutia Urimu na Thumimu[n] ndani ya kifuko hicho. **9** Kisha akakiweka kilemba[o] juu ya kichwa chake na kuweka juu ya kile kilemba upande wa mbele bamba linalong'aa la dhahabu, ile ishara takatifu ya wakfu,[p] kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

10 Sasa Musa akachukua yale mafuta yanayotumiwa kutia mafuta, akaitia mafuta ile maskani[q] na vyote vilivyokuwa ndani yake na kuvitakasa. **11** Kisha akatapanya sehemu yake mara saba kwenye madhabahu na kuitia mafuta madhabahu[r] na vyombo vyake vyote na ile beseni na kinara chake ili kuvitakasa. **12** Mwishowe akamimina sehemu ya mafuta hayo ya kutia mafuta juu ya kichwa cha Haruni na kumtia mafuta ili kumtakasa.[s]

13 Halafu Musa akawaleta karibu wana wa Haruni[t] na kuwavika kanzu na kuwafunga ukumbuu[a] na kuwafunga valio la kichwani,[b] kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

14 Halafu akamwongoza ng'ombe-dume[c] wa toleo la dhambi na Haruni na wanawe wakaweka mikono yao juu ya kichwa[d] cha yule ng'ombe wa toleo la dhambi. **15** Naye Musa akamchinja[e] na kuichukua damu[f] yake na kuitia kwa kidole chake juu ya pembe za madhabahu kuizunguka pande zote na kuitakasa madhabahu kutokana na dhambi, lakini ile damu nyingine akaimimina kwenye msingi wa madhabahu, apate kuitakasa ili afanye upatanisho[g] juu yake. **16** Kisha akachukua mafuta yote yaliyokuwa kwenye matumbo, na kipasho cha ini na figo mbili na mafuta yake naye Musa akayafukiza juu ya madhabahu.[h] **17** Naye akamteketeza kwa moto yule ng'ombe-dume pamoja na ngozi yake na nyama yake na mavi yake nje ya kambi,[i] kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.

18 Sasa akamleta karibu kondoo-dume wa toleo la kuteketezwa, naye Haruni na wanawe wakaweka mikono yao juu ya kichwa cha kondoo huyo.[j] **19** Kisha Musa akamchinja na kuinyunyiza damu yake juu ya madhabahu kuizunguka pande zote.[k] **20** Naye akamkata kondoo huyo vipande-vipande,[l] naye Musa akakifukiza kichwa na vile vipande na yale mafuta. **21** Naye akaosha matumbo na miguu kwa maji, na Musa akamfukiza kondoo mzima juu ya madhabahu.[m] Lilikuwa toleo

SURA 8

a Kut 29:2
b Mdo 7:38
c Hes 27:2
d Kut 36:37
e Yoh 8:28
f Kut 40:12
1Ko 6:11
Efe 5:26
Ebr 9:10
g Kut 29:4
h Kut 28:39
Ufu 19:8
i Kut 39:29
Isa 11:5
j Kut 28:31
Kut 39:22
Hes 15:39
Zb 119:129
k Kut 28:6
Kut 39:2
l Kut 28:8
Kut 29:5
Kut 39:20
m Kut 28:15
Kut 39:9
n Kut 28:30
Ezr 2:63
Yoh 5:30
o Kut 29:6
Kut 39:28
1Ko 11:3
p Kut 28:36
Kut 39:30
q Kut 30:26
r Kut 30:28
s Kut 29:7
Kut 30:30
Kut 40:13
Law 21:10
Zb 133:2
Mdo 10:38
t Kut 29:8
Kut 40:14

Safu ya 2

a Kut 29:9
b Kut 28:40
c Kut 29:10
Law 4:3
Law 16:6
Eze 43:19
d Law 1:4
Law 4:4
e Kut 29:11
f Kut 29:12
Ebr 9:22
g Law 6:7
Law 6:30
h Kut 29:13
Law 4:8
Zb 69:9
i Kut 29:14
Law 4:11
Law 16:27
Ebr 13:12
j Kut 29:15
Law 1:4
k Kut 29:16
l Kut 29:17
m Kut 29:18

la kuteketezwa kwa ajili ya
harufu ya kutuliza.[a] Lilikuwa
toleo linalotolewa kwa Yehova
kwa njia ya moto, kama vile
Yehova alivyokuwa amemwa-
muru Musa.
22 Kisha akamleta karibu
kondoo-dume wa pili, yule ko-
ndoo wa kuweka rasmi,[b] naye
Haruni na wanawe wakaweka
mikono yao juu ya kichwa cha
kondoo huyo. **23** Baada ya
hayo Musa akamchinja na ku-
chukua sehemu ya damu yake
na kuitia kwenye ncha ya si-
kio la kuume la Haruni na kwe-
nye kidole gumba cha mkono
wake wa kuume na kwenye ki-
dole kikubwa cha mguu wake
wa kuume.[c] **24** Kisha Musa
akawaleta karibu wana wa Ha-
runi na kutia sehemu ya damu
kwenye ncha ya sikio lao la
kuume na kwenye kidole gu-
mba chao cha mkono wa kuu-
me na kwenye kidole kikubwa
cha mguu wao wa kuume; laki-
ni Musa akainyunyiza ile damu
iliyobaki juu ya madhabahu
kuizunguka pande zote.[d]
25 Kisha akachukua yale
mafuta na ule mkia mnono na
mafuta yote yaliyokuwa kwe-
nye matumbo,[e] na kipasho cha
ini na zile figo mbili na ma-
futa yake na mguu wa kuu-
me.[f] **26** Na kutoka katika ki-
kapu cha keki zisizo na chachu
kilichokuwa mbele za Yehova
akachukua keki moja ya mvi-
ringo isiyo na chachu[g] na keki
moja ya mviringo ya mkate uli-
otiwa mafuta[h] na mkate mmoja
mwembamba.[i] Halafu akaviwe-
ka juu ya vile vipande vyenye
mafuta na ule mguu wa kuume.
27 Baada ya hayo akaviweka
vyote hivyo juu ya mikono ya
Haruni na mikono ya wanawe
na kuanza kuvitikisa huku na
huku vikiwa toleo la kutikisa
mbele za Yehova.[a] **28** Kisha
Musa akavichukua kutoka mi-
kononi mwao na kuvifukiza
kwenye madhabahu juu ya lile
toleo la kuteketezwa.[b] Hivyo vi-
likuwa dhabihu ya kuweka ra-
smi[c] kwa ajili ya harufu ya
kutuliza.[d] Lilikuwa toleo linalo-
tolewa kwa Yehova kwa njia ya
moto.[e]
29 Naye Musa akachukua ki-
dari[f] na kukitikisa huku na
huku kikiwa toleo la kutikisa
mbele za Yehova.[g] Kutoka ka-
tika yule kondoo-dume wa ku-
weka rasmi kikawa fungu[h] la
Musa, kama vile Yehova alivyo-
kuwa amemwamuru Musa.
30 Baada ya hayo Musa aka-
chukua sehemu ya mafuta ya-
nayotumiwa kutia mafuta[i] na
sehemu ya damu iliyokuwa juu
ya madhabahu na kuvitapanya
juu ya Haruni na mavazi yake
na juu ya wanawe na mavazi ya
wanawe. Basi akamtakasa[j] Ha-
runi na mavazi yake na wana-
we[k] na mavazi ya wanawe.
31 Kisha Musa akamwa-
mbia Haruni na wanawe: "Ito-
koseni[l] nyama kwenye mwi-
ngilio wa hema la mkutano,
na hapo ndipo mtakapoila[m]
na mkate ulio katika kile ki-
kapu cha kuweka rasmi, kama
vile nilivyopewa amri, kuse-
ma, 'Haruni na wanawe wa-
taila.' **32** Na kinachobaki cha
ile nyama na ule mkate mtaki-
teketeza kwa moto.[n] **33** Na-
nyi msitoke nje ya mwingi-
lio wa hema la mkutano kwa
siku saba,[o] mpaka siku ya kuti-
mia kwa siku za kuwekwa kwe-
nu rasmi, kwa sababu itachu-
kua siku saba kuujaza mkono
wenu nguvu.[p] **34** Kama vile

SURA 8
a Mwa 8:21
Efe 5:2
b Kut 29:19
Law 8:33
c Kut 29:20
Law 14:14
Lu 24:44
d Kut 24:6
e Law 3:16
Law 4:9
Law 9:10
Eze 44:7
f Kut 29:22
g Law 2:4
Law 7:12
1Ko 5:8
h Kut 29:2
Hes 6:15
i Kut 29:23

Safu ya 2
a Kut 29:24
Hes 8:13
b Kut 29:25
c Kut 29:19
Law 7:37
d Mwa 8:21
Kut 29:41
Efe 5:2
e Law 1:13
Law 3:5
f Met 23:26
g Kut 29:26
Law 7:30
h Kut 29:27
Law 7:35
i Kut 29:21
Kut 30:30
Zb 99:6
j Kut 29:37
k Hes 3:3
l Kut 29:31
Law 6:28
1Sa 2:13
m Kut 29:32
Law 10:17
1Ko 9:13
Ga 6:6
n Kut 29:34
o Kut 29:30
p Kut 29:35
Hes 3:3

ambavyo imefanywa leo, Yehova ameamuru ifanywe hivyo ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu.[a] **35** Nanyi mtakaa katika mwingilio wa hema la mkutano mchana na usiku kwa siku saba,[b] nanyi mtashika kesha la lazima la Yehova,[c] msije mkafa; kwa maana hivyo ndivyo nimeamriwa.”

36 Naye Haruni na wanawe wakafanya mambo yote ambayo Yehova alikuwa amewaamuru kupitia Musa.

9 Na ikawa kwamba katika siku ya nane,[d] Musa akamwita Haruni na wanawe na wanaume wazee wa Israeli. **2** Kisha akamwambia Haruni: “Jichukulie ndama mchanga awe toleo la dhambi[e] na kondoo-dume awe toleo la kuteketezwa,[f] ambao hawana kasoro, nawe uwatoe mbele za Yehova.[g] **3** Lakini kwa wana wa Israeli utasema, na kuwaambia, ‘Jichukulieni mbuzi-dume[h] kwa ajili ya toleo la dhambi na ndama na mwana-kondoo dume,[i] kila mmoja wao mwenye umri wa mwaka mmoja, ambao hawana kasoro, kwa ajili ya toleo la kuteketezwa, **4** na ng’ombe-dume na kondoo-dume kwa ajili ya dhabihu za ushirika[j] ili uwatoe dhabihu mbele za Yehova, na toleo la nafaka[k] lililotiwa mafuta, kwa sababu leo ndio wakati ambao Yehova atawatokea ninyi.’”[l]

5 Basi wakapeleka vitu ambavyo Musa alikuwa ameamuru mbele ya hema la mkutano. Halafu kusanyiko lote likakaribia na kusimama mbele za Yehova.[m] **6** Naye Musa akasema: “Hili ndilo jambo ambalo Yehova amewaamuru mfanye, ili utukufu wa Yehova uwatokee ninyi.”[a] **7** Halafu Musa akamwambia Haruni: “Nenda karibu na madhabahu, utoe toleo lako la dhambi[b] na toleo lako la kuteketezwa, nawe ufanye upatanisho[c] kwa ajili yako mwenyewe na kwa ajili ya nyumba yako; na utoe toleo la watu[d] na kufanya upatanisho[e] kwa ajili yao, kama vile Yehova alivyoamuru.”

8 Haruni akaenda mara moja karibu na madhabahu na kumchinja yule ndama wa toleo la dhambi aliyekuwa kwa ajili yake.[f] **9** Kisha wana wa Haruni wakampa damu[g] naye akachovya kidole chake katika damu[h] hiyo na kuitia juu ya pembe za madhabahu,[i] na ile damu nyingine iliyobaki akaimimina kwenye msingi wa madhabahu. **10** Naye akafukiza juu ya madhabahu[j] mafuta[k] na figo na kipasho cha ini kutoka katika lile toleo la dhambi, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa. **11** Naye akaiteketeza kwa moto nyama na ngozi nje ya kambi.[l]

12 Kisha akachinja toleo la kuteketezwa nao wana wa Haruni wakampa damu naye akainyunyiza juu ya madhabahu kuizunguka pande zote.[m] **13** Nao wakampa toleo la kuteketezwa likiwa vipande-vipande na kile kichwa, naye akavifukiza juu ya madhabahu.[n] **14** Na zaidi, akaosha matumbo na miguu na kuvifukiza juu ya lile toleo la kuteketezwa kwenye madhabahu.[o]

15 Kisha akatoa lile toleo la watu[p] na kumchukua yule mbuzi wa toleo la dhambi aliyekuwa kwa ajili ya watu na kumchinja na kutoa toleo la dhambi

SURA 8
a Kut 29:36; Law 17:11; Ebr 2:17
b Kut 29:37
c Hes 1:53; Hes 3:7; Kum 11:1; Eze 48:11

SURA 9
d Law 8:35; Eze 43:27
e Law 4:3
f Law 8:18
g Law 8:14
h Law 4:23; Law 16:15; Ezr 6:17
i Law 16:5; Ezr 10:19
j Law 3:1
k Law 2:4; Law 6:14
l Kut 29:43
m Kut 19:17; Kum 31:12

Safu ya 2
a Kut 16:10; Kut 24:16; Kut 40:34; 2Nya 5:14
b Law 4:3
c Law 8:34; Ebr 5:3; Ebr 7:27
d Ebr 5:1
e Law 16:33; Ebr 9:7
f Law 4:4
g Ebr 9:22
h Law 8:15
i Law 4:7; Law 16:18
j Law 8:16
k Law 3:3; Law 4:8
l Law 4:12; Law 8:17; Ebr 13:11
m Law 1:5; Law 8:19
n Law 8:20
o Law 8:21
p Law 4:27; Isa 53:10; Yoh 1:29; 1Ko 15:3; 2Ko 5:21; Ga 1:4; Efe 5:2; Tit 2:14; Ebr 2:17; 1Pe 2:24; 1Yo 2:2

kama yule wa kwanza. **16** Halafu akatoa lile toleo la kuteketezwa na kulitoa kwa kufuatia utaratibu wa kawaida.[a]

17 Kisha akatoa lile toleo la nafaka[b] na kuujaza mkono wake sehemu ya toleo hilo na kulifukiza juu ya madhabahu, mbali na lile toleo la kuteketezwa la asubuhi.[c]

18 Baada ya hayo akamchinja yule ng'ombe-dume na yule kondoo-dume wa dhabihu ya ushirika[d] aliyekuwa kwa ajili ya watu. Halafu wana wa Haruni wakampa damu naye akainyunyiza juu ya madhabahu kuizunguka.[e] **19** Navyo vile vipande vyenye mafuta[f] vya yule ng'ombe-dume na ule mkia mnono[g] wa yule kondoo-dume na yale mafuta yanayofunika na zile figo na kile kipasho cha ini, **20** sasa wakaviweka vile vipande vyenye mafuta juu ya vidari,[h] kisha akavifukiza vipande hivyo vyenye mafuta juu ya madhabahu. **21** Lakini vidari na ule mguu wa kuume, Haruni alivitikisa huku na huku vikiwa toleo la kutikisa[i] mbele za Yehova, kama vile Musa alivyoamuru.

22 Kisha Haruni akainua mikono yake kuelekea watu, akawabariki,[j] naye akashuka[k] baada ya kutoa toleo la dhambi na toleo la kuteketezwa na dhabihu za ushirika. **23** Mwishowe Musa na Haruni wakaingia ndani ya hema la mkutano, kisha wakatoka nje na kuwabariki watu.[l]

Ndipo utukufu wa Yehova[m] ukawatokea watu wote, **24** na moto ukatoka mbele za Yehova[n] nao ukaanza kuteketeza lile toleo la kuteketezwa na vile vipande vyenye mafuta juu ya madhabahu. Watu wote walipoona hilo, wakaanza kupaaza sauti[a] zao nao wakaanguka kifudifudi.

10 Baadaye Nadabu na Abihu,[b] wana wa Haruni, wakachukua na kuleta kila mmoja wao chetezo[c] chake na kutia moto ndani yake na kutia uvumba[d] juu yake, nao wakaanza kumtolea Yehova moto haramu,[e] ambao hakuwa amewaamuru. **2** Ndipo moto ukatoka mbele za Yehova na kuwateketeza,[f] hivi kwamba wakafa mbele za Yehova.[g] **3** Ndipo Musa akamwambia Haruni: "Hivi ndivyo Yehova amesema, 'Na nitakaswe[h] kati ya wale walio karibu nami,[i] nami nitukuzwe mbele ya uso wa watu wote.'"[j] Naye Haruni akakaa kimya.

4 Basi Musa akamwita Mishaeli na Elsafani, wana wa Uzieli,[k] ndugu ya baba ya Haruni, akawaambia: "Njooni karibu, wachukueni ndugu zenu kutoka mbele ya mahali patakatifu mpaka nje ya kambi."[l] **5** Basi wakakaribia na kuwachukua wakiwa na kanzu zao mpaka nje ya kambi, kama vile Musa alivyokuwa amesema.

6 Kwa hiyo Musa akamwambia Haruni na Eleazari na Ithamari wale wanawe wengine: "Msiache vichwa vyenu vikose kuwa nadhifu,[m] wala msiyararue mavazi yenu, msije mkafa wala asije akalikasirikia kusanyiko lote;[n] lakini ndugu zenu wa nyumba yote ya Israeli watalilia kule kuteketeza, ambako Yehova aliteketeza. **7** Nanyi msitoke katika mwingilio wa hema la mkutano msije mkafa,[o] kwa sababu mafuta

SURA 9

a Law 1:3
Law 5:10
Law 6:9
Law 8:18
b Law 2:1
Law 2:4
Law 2:11
Law 2:13
c Kut 29:39
d Law 3:1
Law 7:11
e Law 3:2
f Law 3:3
g Kut 29:22
Law 3:9
Law 8:25
h Law 7:30
i Kut 29:27
Law 8:27
j Hes 6:23
Kum 10:8
Kum 21:5
1Nya 23:13
Lu 24:50
Mdo 3:26
Ebr 7:7
k Kut 20:26
l 2Sa 6:18
2Nya 6:3
m Law 9:6
Hes 14:10
Hes 16:42
n Amu 6:21
1Fa 18:38
1Nya 21:26
2Nya 7:1

Safu ya 2

a 1Fa 18:39
2Nya 7:3

SURA 10

b Kut 6:23
1Nya 24:2
c Kut 27:3
Law 16:12
d Kut 30:35
Law 16:12
e Kut 30:9
Law 10:9
Law 16:2
Isa 28:7
f Hes 16:35
g Law 22:9
Hes 26:61
h Isa 29:23
Eze 20:41
Mt 6:9
i Kut 19:22
Isa 52:11
j Isa 49:3
Yoh 13:31
2Th 1:10
k Kut 6:18
l Mdo 5:6
m Law 21:10
Hes 6:7
n Hes 16:22
Yos 7:1
o Law 21:12

ya Yehova yanayotumiwa kutia mafuta yako juu yenu."[a] Basi wakafanya kulingana na neno la Musa.

8 Naye Yehova akasema na Haruni, na kumwambia: **9** "Usinywe divai wala kileo,[b] wewe na wanao pamoja nawe, mnapoingia ndani ya hema la mkutano, msije mkafa. Hiyo ni sheria mpaka wakati usio na kipimo kwa ajili ya vizazi vyenu, **10** na ili kufanya tofauti kati ya kitu kitakatifu na kile najisi na kati ya kitu kisicho safi na kilicho safi,[c] **11** na ili kuwafundisha wana wa Israeli[d] masharti yote ambayo Yehova amesema kupitia Musa."

12 Ndipo Musa akasema na Haruni na wanawe waliobaki, yaani, Eleazari na Ithamari: "Chukueni toleo la nafaka[e] lililobaki kutoka katika matoleo ya Yehova yaliyotolewa kwa njia ya moto na mle pasipo kutiwa chachu karibu na madhabahu, kwa sababu hilo ni kitu kitakatifu zaidi.[f] **13** Nanyi mtakula katika mahali patakatifu,[g] kwa maana ndilo posho lenu na posho la wana wenu kutoka kwa matoleo ya Yehova yanayotolewa kwa njia ya moto; kwa maana hivyo ndivyo nimeamriwa. **14** Nanyi mtakula kile kidari cha toleo la kutikisa[h] na ule mguu wa lile fungu takatifu[i] katika mahali safi, wewe na wanao na binti zako pamoja nawe,[j] kwa sababu vimetolewa kuwa posho lako na posho la wanao kutoka katika dhabihu za ushirika za wana wa Israeli. **15** Watauleta mguu wa lile fungu takatifu na kile kidari cha toleo la kutikisa[k] pamoja na matoleo yanayotolewa kwa njia ya moto, ya vile vipande vyenye mafuta, ili kutikisa toleo la kutikisa huku na huku, mbele za Yehova; nalo litakuwa posho[a] mpaka wakati usio na kipimo kwa ajili yako na wanao pamoja nawe, kama vile Yehova ameamuru."

16 Naye Musa akamtafuta sana huyo mbuzi wa toleo la dhambi,[b] na, tazama! alikuwa ameteketezwa kabisa. Basi akawaka hasira kuwaelekea Eleazari na Ithamari, wana wa Haruni waliokuwa wamebaki, na kusema: **17** "Kwa nini hamkula lile toleo la dhambi katika mahali palipo patakatifu,[c] kwa kuwa ni kitu kitakatifu zaidi naye amewapa ninyi mpate kujibu kwa ajili ya kosa la kusanyiko ili kufanya upatanisho kwa ajili yao mbele za Yehova?[d] **18** Tazama! damu yake haijaletwa ndani katika mahali patakatifu.[e] Mlipaswa kula toleo hilo katika mahali patakatifu, kama vile nilivyokuwa nimeamriwa."[f] **19** Basi Haruni akasema na Musa: "Tazama! Leo wametoa toleo lao la dhambi na toleo lao la kuteketezwa mbele za Yehova,[g] kisha mambo haya yameanza kunipata; na ikiwa ningekuwa nimekula toleo la dhambi leo, je, jambo hilo lingekuwa jema machoni pa Yehova?"[h] **20** Musa aliposikia hilo, ndipo hilo likawa jema machoni pake.

11 Na Yehova akasema na Musa na Haruni, akiwaambia: **2** "Semeni na wana wa Israeli, na kuwaambia, 'Hiki ndicho kiumbe hai ambacho mnaweza kula[i] kati ya wanyama wote walio kwenye uso wa dunia: **3** Kila kiumbe kati ya wanyama chenye ukwato uliopasuka na chenye mwanya

SURA 10
a Kut 28:41
Law 8:12
b Met 31:5
Isa 28:7
Eze 44:21
Ho 4:11
Efe 5:18
1Ti 3:3
1Ti 3:8
Tit 1:7
c Eze 22:26
Eze 44:23
d Kum 24:8
Kum 33:10
2Nya 17:9
Ne 8:8
Yer 18:18
Mal 2:7
e Kut 29:2
Law 6:16
f Law 21:22
g Law 6:26
Hes 18:10
h Kut 29:26
Law 7:31
Law 9:21
Hes 18:11
i Law 7:34
j Law 22:13
k Law 8:29
Hes 18:18

Safu ya 2
a 1Ko 9:13
b Law 9:3
Law 9:15
c Law 6:26
Law 7:6
Eze 44:29
d Kut 28:38
Hes 18:1
Isa 53:11
Yoh 1:29
2Ko 5:21
Ebr 9:28
1Pe 2:24
e Law 6:30
f Law 6:26
g Law 9:8
Law 9:12
h Law 6:29

SURA 11
i Kum 14:4
Eze 4:14

kwenye ukwato na kinachocheua, hicho ndicho mnachoweza kula.[a]

4 "'Ila hiki ndicho ambacho hamtakula kati ya wacheuaji na wenye ukwato uliopasuka: ngamia, kwa sababu ni mcheuaji lakini hana ukwato uliopasuka. Huyo si safi kwenu.[b] **5** Pia wibari,[c] kwa sababu ni mcheuaji lakini hana ukwato uliopasuka. Huyo si safi kwenu. **6** Pia sungura,[d] kwa sababu ni mcheuaji lakini hana ukwato uliopasuka. Huyo si safi kwenu. **7** Pia nguruwe,[e] kwa sababu ana ukwato uliopasuka naye ana mwanya kwenye ukwato, lakini yeye mwenyewe hacheui. Huyo si safi kwenu. **8** Msile yoyote kati ya nyama zao, wala msiguse mizoga yao.[f] Hao si safi kwenu.[g]

9 "'Hiki ndicho mnachoweza kula kati ya kila kitu kilicho majini:[h] Kila kitu chenye mapezi na magamba[i] majini, katika bahari na katika mito, hivyo mnaweza kula. **10** Na kila kitu katika bahari na katika mito ambacho hakina mapezi na magamba, kati ya kila kiumbe kinachozaana kwa wingi cha majini na kati ya kila nafsi hai iliyo majini, hivyo ni vitu vyenye kuchukiza kwenu. **11** Naam, vitakuwa chukizo kwenu. Msile yoyote kati ya nyama zao,[j] nanyi mtaichukia mizoga yao. **12** Kila kitu majini ambacho hakina mapezi na magamba ni chukizo kwenu.

13 "'Navyo hivi ndivyo mtakavyovichukia kati ya viumbe vinavyoruka.[k] Visiliwe. Hivyo ni chukizo: tai[l] na furukombe na tai-mzoga mweusi, **14** na mwewe mwekundu na mwewe mweusi[m] kulingana na aina yake, **15** na kila kunguru[a] kulingana na aina yake, **16** na mbuni[b] na bundi na shakwe na kipanga kulingana na aina yake, **17** na bundi mdogo na mnandi na bundi mwenye masikio marefu,[c] **18** na batamaji na mwari na tai-mzoga,[d] **19** na korongo, kulastara kulingana na aina yake na hudihudi na popo.[e] **20** Kila kiumbe chenye mabawa kinachozaana kwa wingi ambacho hutembea kwa miguu minne ni chukizo kwenu.[f]

21 "'Ila hiki ndicho mnachoweza kula kati ya viumbe vyote vyenye mabawa vinavyozaana kwa wingi ambavyo hutembea kwa miguu minne, vile vyenye miguu ya kuruka juu ya miguu yao, ili kuruka nayo juu ya dunia. **22** Hawa ndio mnaoweza kula kati yao: nzige mwenye kuhama[g] kulingana na aina yake, na nzige anayeweza kuliwa[h] kulingana na aina yake, na nyenje kulingana na aina yake na panzi[i] kulingana na aina yake. **23** Na kila kiumbe kingine chenye mabawa kinachozaana kwa wingi chenye miguu minne ni chukizo[j] kwenu. **24** Basi kupitia kwao mtajifanya wenyewe msiwe safi. Kila mtu anayegusa mizoga yao atakuwa asiye safi mpaka jioni.[k] **25** Na kila mtu anayebeba wowote kati ya mizoga yao atayafua[l] mavazi yake, naye atakuwa asiye safi mpaka jioni.

26 "'Na mnyama yeyote ambaye ana ukwato uliopasuka lakini hana mwanya wala si mcheuaji, hao si safi kwenu. Kila mtu anayewagusa hao atakuwa si safi.[m] **27** Na kila kiumbe kinachotembea kwa miguu yenye makucha kati ya vi-

SURA 11

a Kum 14:6
b Kum 14:7
c Zb 104:18
Met 30:26
d Kum 14:7
e Kum 14:8
Isa 65:4
Isa 66:3
Isa 66:17
f Law 11:24
g Mdo 10:14
h Kum 14:9
i Mt 4:18
Lu 24:42
j Kum 14:3
Kum 14:10
k Kum 14:12
l Ayu 39:30
Mt 24:28
m Kum 14:13

Safu ya 2

a Kum 14:14
b Kum 14:15
c Kum 14:16
d Kum 14:17
e Kum 14:18
f Kum 14:19
g Kut 10:12
Met 30:27
Isa 33:4
h Mt 3:4
Mk 1:6
i 2Nya 7:13
j Kum 14:3
k Law 17:15
l Kut 19:10
Law 14:8
Law 15:5
Hes 19:10
m Kum 14:8

umbe hai vinavyoenda kwa miguu minne, hao si safi kwenu. Kila mtu anayeigusa mizoga yao atakuwa asiye safi mpaka jioni. **28** Naye anayeibeba mizoga[a] yao atafua mavazi yake,[b] naye atakuwa asiye safi mpaka jioni. Hao si safi kwenu.

29 "'Nacho hiki ndicho kisicho safi kwenu kati ya viumbe vinavyozaana kwa wingi ambavyo hujaa duniani:[c] fuko na panya anayeruka[d] na mjusi kulingana na aina yake, **30** na mjusi kafiri na mjusi mkubwa na mjusi wa majini na mjusi wa mchangani na kinyonga. **31** Hao si safi kwenu kati ya viumbe vyote vinavyozaana kwa wingi.[e] Kila mtu anayevigusa viumbe hivyo vikiwa vimekufa atakuwa asiye safi mpaka jioni.[f]

32 "'Sasa chochote ambacho yeyote kati yao ataangukia akiwa amekufa kitakuwa kisicho safi, kiwe ni chombo cha mbao[g] au nguo au ngozi[h] au nguo ya gunia.[i] Chombo chochote ambacho hutumiwa kwa njia fulani kitatiwa katika maji, nacho kitakuwa kisicho safi mpaka jioni halafu kitakuwa safi. **33** Nacho chombo chochote cha udongo[j] ambacho yeyote kati yao ataanguka ndani yake, chochote kilicho ndani yake kitakuwa kisicho safi, nanyi mtakivunja.[k] **34** Chakula cha namna yoyote ambacho huenda kikaliwa kitakachopata maji kutoka katika chombo hicho kitakuwa kisicho safi, na kinywaji chochote ambacho kinaweza kunywewa katika chombo chochote kitakuwa kisicho safi. **35** Na kila kitu ambacho juu yake huenda wowote kati ya mizoga yao ukaangukia kitakuwa kisicho safi. Iwe ni jiko au kinara cha mtungi, kitavunjwa. Vitu hivyo si safi, navyo vitakuwa si safi kwenu. **36** Ila tu bubujiko na shimo la maji yaliyozuiliwa ndiyo yatakayoendelea kuwa safi, lakini mtu yeyote anayegusa mizoga yao atakuwa asiye safi. **37** Na wowote wa mizoga ukianguka juu ya mbegu yoyote ya mmea wa kupandwa, ni safi. **38** Lakini ikiwa maji yatatiwa juu ya mbegu na kitu fulani cha mizoga yao kianguke juu yake, si safi kwenu.

39 "'Sasa, ikiwa mnyama yeyote aliye wenu kwa ajili ya chakula atakufa, mtu anayeugusa mzoga wake atakuwa asiye safi mpaka jioni.[a] **40** Naye anayekula[b] sehemu yoyote ya mzoga wake atayafua mavazi yake, naye atakuwa asiye safi mpaka jioni; naye anayeubeba mzoga wake atayafua mavazi yake, naye atakuwa asiye safi mpaka jioni. **41** Na kila kiumbe kinachozaana kwa wingi ambacho kinajaa duniani ni chukizo.[c] Kisiliwe. **42** Nacho kiumbe chochote ambacho hutembea kwa tumbo[d] na kiumbe chochote ambacho hutembea kwa miguu yote minne au hesabu yoyote kubwa ya miguu ya viumbe vyote vinavyozaana kwa wingi ambavyo vinajaa duniani, msivile, kwa sababu hivyo ni chukizo.[e] **43** Msifanye nafsi zenu ziwe zenye kuchukiza kutokana na kiumbe chochote kinachozaana kwa wingi ambacho kinajaa, wala msijifanye kuwa wasio safi kutokana nao na kupata kuwa wasio safi kutokana nao.[f] **44** Kwa maana mimi ni Yehova Mungu wenu;[g] nanyi mtajitakasa

SURA 11

a Law 5:2
b Law 17:16
c Ebr 9:10
d Isa 66:17
e Law 22:5
Kum 14:19
f Law 11:24
g Kut 7:19
h Mwa 21:14
i Mwa 37:34
j Law 6:28
Mk 14:13
k Law 15:12
Isa 30:14

Safu ya 2

a Law 11:24
Hes 19:11
Hes 19:16
b Law 17:15
Law 22:8
Kum 14:21
Eze 4:14
Eze 44:31
Mdo 10:13
c Law 11:21
d Mwa 3:14
Mik 7:17
e Kum 14:3
f Law 20:25
g Kut 20:2
Kum 5:6

wenyewe nanyi mtakuwa wa-
takatifu,[a] kwa sababu mimi
ni mtakatifu.[b] Kwa hiyo msi-
fanye nafsi zenu kuwa zisizo
safi kutokana na kiumbe cho-
chote kinachozaana kwa wi-
ngi ambacho hutembea juu ya
dunia. **45** Kwa maana mimi
ni Yehova anayewaongoza ni-
nyi kutoka katika nchi ya Mi-
sri ili kujionyesha kuwa Mungu
kwenu;[c] nanyi mtakuwa wata-
katifu,[d] kwa sababu mimi ni
mtakatifu.[e]

46 "'Hiyo ndiyo sheria juu ya
mnyama na kiumbe kinacho-
ruka na kila nafsi hai amba-
yo hutembea majini[f] na kuhu-
su kila nafsi inayojazana duni-
ani, **47** ili kufanya tofauti[g] kati
ya kisicho safi na kilicho safi na
kati ya kiumbe hai kinachowe-
za kuliwa na kiumbe hai kisi-
chopasa kuliwa.'"

12 Naye Yehova akaendelea
kusema na Musa, na ku-
mwambia: **2** "Sema na wana
wa Israeli, na kuwaambia, 'Iki-
wa mwanamke atachukua mi-
mba[h] na kuzaa mtoto wa kiu-
me, atakuwa asiye safi kwa
siku saba; kama vile katika
siku za uchafu wakati anapo-
kuwa na hedhi atakuwa asiye
safi.[i] **3** Na siku ya nane ngo-
zi ya govi la mtoto huyo ita-
tahiriwa.[j] **4** Kwa siku 33 zai-
di mwanamke huyo atakaa ka-
tika damu ya utakaso. Asiguse
kitu chochote kilicho kitakati-
fu, wala asiingie mahali pata-
katifu mpaka kutimia kwa siku
za utakaso wake.[k]

5 "'Sasa, ikiwa atazaa mtoto
wa kike, basi atakuwa asiye safi
kwa siku 14, kama vile waka-
ti wa kuwa na hedhi. Kwa siku
66 zaidi atakaa katika damu
ya utakaso wake. **6** Kisha zi-

SURA 11
a Kut 19:6
Law 19:2
Kum 14:2
1Th 4:7
1Pe 1:15
b 1Pe 1:16
Ufu 4:8
c Mwa 46:4
Kut 6:7
Kut 29:46
Zb 81:10
Ho 11:1
d Kut 22:31
Law 20:7
Law 20:26
Hes 15:40
Kum 7:6
e Yos 24:19
1Sa 2:2
1Sa 6:20
f Mwa 1:21
g Law 10:10
Law 20:25
Eze 22:26
Eze 44:23

SURA 12
h Mwa 4:1
i Law 15:19
j Mwa 17:12
Mwa 21:4
Lu 1:59
Lu 2:21
Yoh 7:22
k Lu 2:22

Safu ya 2
a Law 1:4
Law 1:10
b Law 15:14
c Law 15:28
d Law 1:14
Law 5:7
Law 14:22
Lu 2:24
e Law 4:26
Law 6:7
Hes 15:25

SURA 13
f Law 14:56
g Hes 12:10
2Nya 26:19
Mt 8:3
h Kum 24:8
Mal 2:7
Lu 17:14
i Law 10:10
Eze 44:23

takapotimia siku za utakaso
wake kwa ajili ya mwana au
binti ataleta mwana-kondoo
dume katika mwaka wake wa
kwanza kwa ajili ya toleo la
kuteketezwa[a] na hua mchanga
au njiwa-tetere[b] kwa ajili ya to-
leo la dhambi kwenye mwingi-
lio wa hema la mkutano kwa
kuhani. **7** Naye atalitoa mbe-
le za Yehova na kufanya upata-
nisho kwa ajili ya mwanamke
huyo, naye atakuwa safi kuto-
kana na chemchemi ya damu
yake.[c] Hiyo ndiyo sheria juu
ya mwanamke anayezaa mtoto
wa kiume au wa kike. **8** Laki-
ni ikiwa hana uwezo wa kuto-
sha wa kutoa kondoo, basi ata-
chukua njiwa-tetere wawili au
hua wachanga wawili,[d] mmoja
kwa ajili ya toleo la kuketete-
zwa na yule mwingine kwa ajili
ya toleo la dhambi, naye kuhani
atafanya upatanisho[e] kwa ajili
yake, naye atakuwa safi.'"

13 Na Yehova akasema na
Musa na Haruni, na ku-
waambia: **2** "Ikiwa ngozi ya
mwili wa mtu itatokeza upe-
le au kigaga[f] au doa na kukua
katika ngozi ya mwili wake na
kuwa pigo la ukoma,[g] basi atale-
twa kwa Haruni kuhani au kwa
mmoja wa wanawe walio ma-
kuhani.[h] **3** Naye kuhani ata-
liangalia lile pigo lililo kati-
ka ngozi ya mwili.[i] Nywele zi-
lizo katika pigo hilo zikigeuka
na kuwa nyeupe na pigo lione-
kane kuwa limepenya chini ya
ngozi ya mwili wake, ni pigo
la ukoma. Naye kuhani atalita-
zama, naye atamtangaza kuwa
asiye safi. **4** Lakini ikiwa doa
ni jeupe katika ngozi ya mwi-
li wake nalo halionekani kuwa
limepenya chini ya ngozi yake
na nywele zake hazijageuka na

kuwa nyeupe, basi kuhani atamtenga[a] mwenye pigo hilo siku saba. **5** Naye kuhani atamtazama siku ya saba, na ikiwa pigo hilo linaonekana kuwa limekoma, pigo hilo halijaenea katika ngozi, kuhani atamtenga[b] pia siku nyingine saba.

6 "Naye kuhani atamtazama katika siku ya saba mara ya pili, na ikiwa pigo limefifia nalo pigo halijaenea katika ngozi, kuhani atamtangaza pia kuwa safi. Lilikuwa kigaga. Naye atayafua mavazi yake na kuwa safi. **7** Lakini ikiwa pasipo shaka kigaga hicho kimeenea katika ngozi baada ya kuonekana mbele ya kuhani ili kuthibitisha utakaso wake, basi atajionyesha tena mara ya pili mbele ya kuhani,[c] **8** naye kuhani atatazama; na ikiwa kigaga hicho kimeenea katika ngozi, basi kuhani huyo atamtangaza kuwa asiye safi. Ni ukoma.[d]

9 "Ikiwa pigo la ukoma litatokea katika mtu, ataletwa kwa kuhani. **10** Naye kuhani atatazama;[e] na ikiwa kuna upele mweupe katika ngozi nao umegeuza nywele kuwa nyeupe na ubichi wa nyama iliyo hai[f] upo kwenye upele huo, **11** huo ni ukoma wa kudumu[g] katika ngozi ya mwili wake; naye kuhani atamtangaza kuwa asiye safi. Hapaswi kumtenga,[h] kwa kuwa yeye si safi. **12** Sasa ikiwa pasipo shaka ukoma huo unatokea katika ngozi, nao ukoma ufunike ngozi yote ya mtu mwenye pigo hilo toka kichwani pake mpaka miguuni pake na kuonekana kikamili machoni pa kuhani; **13** naye kuhani ametazama nao ukoma umeufunika mwili wake wote, basi atalitangaza pigo hilo kuwa safi.

SURA 13

a Law 14:38
Hes 12:15

b Law 14:46

c Law 13:27

d Hes 12:12

e Law 13:3
2Nya 26:20

f Law 13:24

g 2Nya 26:21

h Law 13:4

Safu ya 2

a Kum 24:8

b Law 13:8

c Lu 5:14
Lu 17:14

d Kum 28:27
2Fa 20:7
Ayu 2:7

e Law 10:10
Eze 44:23

f Law 13:4
Law 14:38
Hes 12:15

g Kum 28:22

h Lu 5:14
Lu 17:14

Lote limegeuka kuwa jeupe. Yeye ni safi. **14** Lakini siku ambayo nyama mbichi itaonekana ndani yake, atakuwa najisi. **15** Naye kuhani[a] ataiona nyama hai, naye atamtangaza kuwa asiye safi. Hiyo nyama hai si safi. Ni ukoma.[b] **16** Au ikiwa nyama hai itarudi na kubadilika kuwa nyeupe, ndipo atakuja kwa kuhani. **17** Naye kuhani atamtazama,[c] na ikiwa pigo hilo limebadilika na kuwa jeupe, ndipo kuhani atalitangaza pigo hilo kuwa safi. Yeye ni safi.

18 "Na kuhusu nyama, ikiwa jipu[d] litatokea katika ngozi yake nalo lipone, **19** na mahali pa jipu patokee upele mweupe au doa jekundu-jeupe, ndipo atajionyesha kwa kuhani. **20** Naye kuhani atatazama,[e] na ikiwa linaonekana kuwa limepenya chini ya ngozi na nywele zake zimegeuka na kuwa nyeupe, ndipo kuhani atamtangaza kuwa asiye safi. Ni pigo la ukoma. Limetokea katika jipu. **21** Lakini kuhani akilitazama, na, tazama sasa, hakuna nywele nyeupe ndani yake wala halijapenya chini ya ngozi na limefifia, kuhani atamtenga[f] siku saba. **22** Na ikiwa pasipo shaka limeenea katika ngozi, ndipo kuhani huyo atamtangaza kuwa asiye safi. Ni pigo. **23** Lakini doa likibaki mahali pake, halijaenea, ni jipu lenye kuwasha;[g] naye kuhani atamtangaza kuwa safi.[h]

24 "Au ikiwa ngozi ya mwili itakuwa na kovu kutokana na moto, na ubichi wa nyama wa kovu hilo uwe doa jekundu-jeupe au jeupe, **25** ndipo kuhani atalitazama; na ikiwa nywele zimegeuka na kuwa nyeupe

katika doa hilo nalo linaonekana kuwa limepenya chini ya ngozi, ni ukoma. Umetokea katika kovu hilo, naye kuhani atamtangaza kuwa asiye safi. Ni pigo la ukoma. **26** Lakini ikiwa kuhani ataliangalia, na, tazama sasa, hakuna nywele nyeupe katika doa hilo nalo halijapenya chini ya ngozi nalo limefifia, ndipo kuhani atamtenga siku saba. **27** Naye kuhani atamtazama katika siku ya saba. Ikiwa pasipo shaka limeenea katika ngozi, ndipo kuhani atamtangaza kuwa asiye safi. Ni pigo la ukoma. **28** Lakini doa hilo likibaki mahali pake, halijaenea katika ngozi nalo limefifia, ni upele wa kovu; naye kuhani atamtangaza kuwa safi, kwa sababu ni kovu lenye kuwasha.

29 "Na mwanamume au mwanamke, ikiwa atapata pigo kwenye kichwa au kwenye kidevu, **30** ndipo kuhani[a] ataliona pigo hilo; na ikiwa linaonekana kuwa limepenya chini ya ngozi, nazo nywele ni za manjano na ni chache ndani yake, ndipo kuhani atamtangaza kuwa asiye safi. Ni kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida.[b] Ni ukoma wa kichwa au wa kidevu. **31** Lakini ikiwa kuhani ataliona pigo la kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida, na, tazama! linaonekana kuwa halijapenya chini ya ngozi wala hakuna nywele nyeusi hapo, ndipo kuhani atamtenga[c] mwenye pigo la kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida kwa siku saba.[d] **32** Naye kuhani atalitazama pigo hilo katika siku ya saba; na ikiwa kule kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida hakujaenea, wala hakuna nywele za manjano ambazo zimekuwa hapo na kule kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida[a] hakujapenya chini ya ngozi, **33** ndipo atanyolewa, lakini hatapanyoa mahali palipoanguka nywele isivyo kawaida;[b] naye kuhani atamtenga siku nyingine saba huyo mtu ambaye nywele zimeanguka isivyo kawaida.

34 "Naye kuhani atatazama kule kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida katika siku ya saba; na ikiwa kule kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida hakujaenea katika ngozi, wala haionekani kwamba kumepenya chini ya ngozi, ndipo kuhani atamtangaza kuwa safi,[c] naye atayafua mavazi yake na kuwa safi. **35** Lakini ikiwa pasipo shaka kule kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida kunaenea katika ngozi baada ya kuthibitishwa kwa utakaso wake, **36** ndipo kuhani[d] atamwona; na ikiwa kule kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida kumeenea katika ngozi, kuhani hana haja ya kuchunguza nywele za manjano; yeye si safi. **37** Lakini ikiwa kwa kuonekana kwake, kule kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida kumesimama na nywele nyeusi zimeota hapo, kule kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida kumepona. Yeye ni safi, naye kuhani atamtangaza kuwa safi.[e]

38 "Na mwanamume au mwanamke, ikiwa madoa[f] yatatokea katika ngozi ya mwili wao, madoa meupe, **39** ndipo kuhani[g] atatazama; na ikiwa madoa hayo katika ngozi ya mwili wao ni ya rangi nyeupe

SURA 13

a Kum 24:8
Mal 2:7

b Law 14:54

c Law 14:38
Hes 12:15

d Law 13:4

Safu ya 2

a Law 14:54

b Law 14:8

c Law 13:23
Mk 1:42
Lu 5:13

d Eze 22:26
Lu 17:14

e Mt 8:4
Mk 1:44

f Law 13:2

g Law 10:10

iliyofifia, ni upele usio na madhara. Umetokea katika ngozi. Yeye ni safi.

40 "Naye mwanamume, ikiwa kichwa chake kitaanza kuwa na upara,[a] ni upara. Yeye ni safi. **41** Na ikiwa kichwa chake kitakuwa na upara upande wa mbele, ni upara wa paji la uso. Yeye ni safi. **42** Lakini ikiwa pigo jekundu-jeupe litatokea katika upara wa utosi au wa paji la uso, ni ukoma unaotokea katika upara wa utosi wake au paji lake la uso. **43** Naye kuhani[b] atamtazama; na ikiwa kuna upele wa pigo jekundu-jeupe katika upara wa utosi wake au wa paji lake la uso unaoonekana kama ukoma katika ngozi ya mwili, **44** yeye ni mwenye ukoma. Yeye si safi. Kuhani atamtangaza kuwa asiye safi. Pigo lake lipo kichwani pake. **45** Naye mwenye ukoma ambaye ana pigo ndani yake, mavazi yake yatararuliwa,[c] na kichwa chake kisitunzwe,[d] naye anapaswa kufunika masharubu[e] yake na kupaaza sauti, 'Si safi, si safi!'[f] **46** Siku zote ambazo pigo hilo litakuwa ndani yake atakuwa si safi. Yeye si safi. Atakaa akiwa ametengwa. Makao yake yatakuwa nje ya kambi.[g]

47 "Kwa habari ya vazi, ikiwa pigo la ukoma litatokea ndani yake, iwe ni ndani ya vazi la sufu au ni ndani ya vazi la kitani, **48** au ndani ya mtande[h] au ndani ya mshindio wa kitani na wa sufu, au ndani ya ngozi au ndani ya chochote kilichotengenezwa kwa ngozi,[i] **49** nalo pigo la rangi ya kijani-manjano au la rangi nyekundu-nyekundu litokee ndani ya vazi hilo au ndani ya ngozi au ndani ya mtande au ndani ya mshindio au ndani ya chombo chochote cha ngozi, ni pigo la ukoma, nalo lazima lionyeshwe kwa kuhani. **50** Naye kuhani[a] ataona pigo hilo, naye atalitenga[b] pigo hilo siku saba. **51** Atakapokuwa ameliona pigo hilo katika siku ya saba, ya kwamba pigo hilo limeenea katika vazi au katika mtande au katika mshindio[c] au katika ngozi ambayo inaweza kutumiwa kwa ajili ya matumizi yoyote, pigo hilo ni ukoma hatari.[d] Si safi. **52** Naye atateketeza vazi hilo au mtande huo au mshindio huo katika sufu hiyo au katika kitani[e] hicho, au chombo chochote cha ngozi ambamo pigo hilo linaweza kutokea, kwa sababu ni ukoma hatari.[f] Utateketezwa katika moto.

53 "Lakini ikiwa kuhani anatazama, na, tazama sasa, pigo hilo halijaenea katika vazi au katika mtande au katika mshindio au katika chombo chochote cha ngozi,[g] **54** kuhani pia ataamuru waoshe kile ambacho ndani yake mna pigo hilo, naye atalitenga mara ya pili kwa siku saba. **55** Naye kuhani atatazama pigo hilo baada ya kuoshwa, na ikiwa kuonekana kwa pigo hilo hakujabadilika na bado pigo hilo halijaenea, si safi. Utaliteketeza katika moto. Ni tundu lililo chini katika kiraka kilichochanika upande wa ndani au wa nje.

56 "Lakini ikiwa kuhani ametazama, na, tazama sasa, pigo limefifia baada ya kuoshwa, ndipo atalirarua kutoka katika vazi au ngozi au mtande au mshindio. **57** Hata hivyo, ikiwa bado linaonekana katika vazi au katika mtande au

SURA 13

a 2Fa 2:23

b Eze 44:23

c 2Sa 13:19
Ezr 9:5

d Law 10:6
Law 21:10

e Eze 24:17
Mik 3:7

f Omb 4:15

g Hes 5:2
Hes 12:14
2Fa 7:3
2Nya 26:21

h Law 13:53
Law 13:59

i Mwa 21:15
Law 13:53
Mk 2:22

Safu ya 2

a Law 10:10
Eze 44:23

b Law 13:4

c Law 13:58

d Law 14:44

e Kut 28:39
Kut 39:28

f Law 14:44

g Mwa 3:21
Mwa 21:14
Eze 16:10
Mt 3:4

katika mshindio[a] au katika chombo chochote cha ngozi, linatokea. Utakiteketeza[b] motoni chochote kile ambacho ndani yake mna pigo hilo. **58** Nalo vazi au mtande au mshindio au chombo chochote cha ngozi ambacho utaosha, pigo litakapokuwa limetoweka kutoka kwake, kitaoshwa tena mara ya pili; nacho kitakuwa safi.

59 "Hiyo ndiyo sheria ya pigo la ukoma katika vazi la sufu au kitani,[c] au katika mtande au katika mshindio, au katika chombo chochote cha ngozi, ili kukitangaza kuwa safi au kukitangaza kuwa si safi."

14 Na Yehova akaendelea kusema na Musa, na kumwambia: **2** "Hii itakuwa sheria ya mwenye ukoma[d] katika siku ya kuthibitisha utakaso wake, atakapoletwa kwa kuhani.[e] **3** Naye kuhani atatoka nje ya kambi, na kuhani atatazama; na ikiwa pigo la ukoma limepona[f] katika yule mwenye ukoma, **4** ndipo kuhani atatoa amri; naye atachukua ndege wawili walio safi[g] na mti wa mwerezi[h] na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili[i] na hisopo[j] ili kujitakasa. **5** Naye kuhani atatoa amri, na yule ndege mmoja atauawa katika chombo cha udongo juu ya maji yanayotiririka.[k] **6** Naye yule ndege aliye hai, atamchukua na huo mti wa mwerezi na kile kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na hisopo, naye atavichovya pamoja na yule ndege aliye hai katika damu ya huyo ndege aliyeuawa juu ya maji yanayotiririka. **7** Kisha ataitapanya[l] mara saba[m] juu ya yule anayejitakasa kutokana na ukoma naye atamtangaza kuwa safi,[a] naye atamwachilia ndege aliye hai aruke kwenda zake porini.[b]

8 "Na yule anayejitakasa atayafua mavazi[c] yake na kunyoa nywele zake zote na kuoga[d] katika maji naye atakuwa safi, kisha baadaye ataingia kambini. Naye atakaa nje ya hema lake kwa siku saba.[e] **9** Na itakuwa kwamba katika siku ya saba atanyoa nywele zake zote zilizo kichwani[f] pake na kwenye kidevu chake na nyusi zake. Naam, atanyoa nywele zake zote, naye atayafua mavazi yake na kuoga mwili wake katika maji; naye atakuwa safi.

10 "Na katika siku ya nane[g] atachukua wana-kondoo dume wawili ambao hawana kasoro na mwana-kondoo jike mmoja ambaye hana kasoro,[h] katika mwaka wake wa kwanza, na sehemu tatu za kumi za efa ya unga laini kuwa toleo la nafaka[i] lililotiwa mafuta na logi moja ya mafuta;[j] **11** na kuhani anayemtangaza kuwa safi atamleta mtu huyo anayejitakasa, na vitu hivyo, mbele za Yehova katika mwingilio wa hema la mkutano. **12** Naye kuhani atamchukua yule mwana-kondoo dume na kumtoa kwa ajili ya toleo la hatia[k] pamoja na ile logi[l] moja ya mafuta naye atavitikisa huku na huku kama toleo la kutikisa[m] mbele za Yehova. **13** Naye atamchinja yule mwana-kondoo dume mahali[n] ambapo lile toleo la dhambi na toleo la kuteketezwa huchinjiwa kwa kawaida, katika mahali patakatifu,[o] kwa sababu, kama vile toleo la dhambi, vivyo hivyo toleo la hatia ni la kuhani.[p] Ni kitu kitakatifu zaidi.

SURA 13
a Law 13:48
b Law 13:52
c Law 13:47

SURA 14
d Law 13:2
e Mk 1:44
Lu 5:14
f Lu 7:22
Lu 17:15
g Law 1:14
Law 14:30
Law 14:49
h Hes 19:6
i Ebr 9:19
j Kut 12:22
Law 14:51
Hes 19:18
1Fa 4:33
Zb 51:7
k Law 14:50
Law 15:13
l Ebr 9:13
m 2Fa 5:10

Safu ya 2
a Law 13:23
b Law 16:22
Zb 103:12
c Law 13:6
d Law 15:6
e Law 13:5
Hes 5:2
Hes 12:15
f Law 13:33
g Law 15:14
h Law 4:32
i Law 2:1
j Mk 1:44
k Law 5:2
Law 6:6
l Law 14:24
m Kut 29:24
Law 7:30
Hes 8:11
n Law 1:11
Law 4:4
Law 6:25
o Law 7:6
p Law 2:3
Law 7:7
1Ko 9:13
1Ko 10:18

14 "Naye kuhani atachukua
sehemu ya damu ya toleo la ha-
tia, naye kuhani ataitia kwe-
nye ncha ya sikio la kuume
la yule anayejitakasa na kwe-
nye kidole gumba cha mkono
wake wa kuume na kwenye ki-
dole kikubwa cha mguu wake
wa kuume.[a] **15** Naye kuhani
atachukua kiasi fulani cha ile
logi[b] ya mafuta na kuyamimina
kwenye kiganja cha mkono wa
kushoto wa kuhani. **16** Naye
kuhani atachovya kidole chake
cha kuume ndani ya mafuta ya-
liyo katika mkono wake wa ku-
shoto naye atatapanya sehe-
mu ya mafuta hayo kwa kido-
le chake mara saba[c] mbele za
Yehova. **17** Nayo yale mafuta
mengine yaliyo kwenye mkono
wake atatia sehemu yake kwe-
nye ncha ya sikio la yule anaye-
jitakasa na kwenye kidole gu-
mba cha mkono wake wa kuu-
me na kwenye kidole kikubwa
cha mguu wake wa kuume juu
ya ile damu ya toleo la hatia.[d]
18 Na mafuta yanayobaki ya-
liyo kwenye mkono wa kuha-
ni atayatia kwenye kichwa cha
yule anayejitakasa, naye ku-
hani atafanya upatanisho[e] kwa
ajili yake mbele za Yehova.

19 "Naye kuhani atatoa to-
leo la dhambi[f] na kufanya upa-
tanisho kwa ajili ya yule anaye-
jitakasa kutokana na uchafu
wake, na baadaye atachinja
lile toleo la kuteketezwa.
20 Naye kuhani atatoa toleo la
kuteketezwa na toleo la nafaka[g]
juu ya madhabahu, naye ku-
hani[h] atafanya upatanisho kwa
ajili yake;[i] naye atakuwa safi.[j]

21 "Hata hivyo, ikiwa yeye
ni wa hali ya chini[k] naye hana
mapato ya kutosha,[l] basi ata-
chukua mwana-kondoo dume
mmoja akiwa toleo la hatia
kwa ajili ya toleo la kutikisa
ili kufanya upatanisho kwa aji-
li yake na sehemu ya kumi
ya efa ya unga laini uliotiwa
mafuta ukiwa toleo la nafaka
na logi ya mafuta, **22** na nji-
wa-tetere[a] wawili au hua wawili
wachanga, kulingana na mapa-
to yake, na mmoja atakuwa to-
leo la dhambi na yule mwingine
atakuwa toleo la kuteketezwa.
23 Na siku ya nane[b] atawaleta
ili kuthibitisha utakaso[c] wake
kwa kuhani katika mwingilio
wa hema la mkutano[d] mbele za
Yehova.

24 "Naye kuhani atamchu-
kua yule mwana-kondoo dume
wa toleo la hatia[e] na ile logi
ya mafuta, naye kuhani atavi-
tikisa huku na huku vikiwa to-
leo la kutikisa mbele za Yeho-
va.[f] **25** Naye atamchinja yule
kondoo-dume mchanga wa to-
leo la hatia, naye kuhani ata-
chukua sehemu ya damu ya to-
leo la hatia na kuitia kwenye
ncha ya sikio la kuume la yule
anayejitakasa na kwenye kido-
le gumba cha mkono wake wa
kuume na kwenye kidole ki-
kubwa cha mguu wake wa ku-
ume.[g] **26** Naye kuhani atami-
mina sehemu ya mafuta hayo
kwenye kiganja cha mkono wa
kushoto wa kuhani.[h] **27** Naye
kuhani atatapanya[i] kwa kido-
le chake cha kuume sehemu
ya mafuta yaliyo katika mko-
no wake wa kushoto mara saba
mbele za Yehova. **28** Naye ku-
hani atatia sehemu ya mafuta
hayo yaliyo katika mkono wake
kwenye ncha ya sikio la kuume
la yule anayejitakasa na kwe-
nye kidole gumba cha mkono
wake wa kuume na kwenye ki-
dole kikubwa cha mguu wake

SURA 14
a Kut 29:20
b Law 14:10
Law 14:24
c Law 4:6
Law 4:17
d Law 8:24
e Law 6:7
1Yo 1:7
1Yo 2:2
f Law 5:6
g Law 2:1
Law 14:10
Hes 15:4
h Law 4:26
Law 10:10
Ebr 2:17
i Mt 8:4
Lu 5:14
j Law 14:9
k Zb 72:13
Met 17:5
Met 22:2
Lu 6:20
l Law 5:7
Law 12:8

Safu ya 2
a Law 1:14
b Law 15:13
Law 15:14
Hes 12:14
c Law 14:2
Law 14:7
d Law 14:11
e Law 5:2
Law 6:6
f Law 14:12
g Law 8:23
Law 14:14
h Law 14:15
i Law 14:7

wa kuume juu ya mahali pe-
nye ile damu ya toleo la hatia.[a]
29 Na yatakayobaki kati ya
yale mafuta yaliyo katika mko-
no wa kuhani, atayatia kwenye
kichwa[b] cha yule anayejitakasa
ili kufanya upatanisho kwa aji-
li yake mbele za Yehova.

30 "Naye atamtoa mmoja wa
wale njiwa-tetere au wa wale
hua wachanga anaoweza kuwa-
pata,[c] **31** mmoja wa hao anao-
weza kuwapata akiwa toleo la
dhambi[d] na yule mwingine aki-
wa toleo la kuteketezwa[e] pamo-
ja na toleo la nafaka; naye ku-
hani atafanya upatanisho[f] kwa
ajili ya yule anayejitakasa mbe-
le za Yehova.

32 "Hiyo ndiyo sheria kwa
ajili ya yule aliyekuwa na pigo
la ukoma ambaye huenda asiwe
na uwezo wakati wa kuthibiti-
sha utakaso wake."

33 Naye Yehova akasema na
Musa na Haruni, na kuwaam-
bia: **34** "Mtakapoingia kati-
ka nchi ya Kanaani,[g] ambayo
ninawapa ninyi iwe mali yenu,[h]
nami niweke pigo la ukoma ka-
tika nyumba ya nchi mtakayo-
imiliki,[i] **35** basi mwenye nyu-
mba hiyo atakuja na kumwa-
mbia kuhani, na kusema, 'Kitu
fulani kama pigo kimenitokea
katika nyumba.' **36** Naye ku-
hani atatoa maagizo, nao wata-
ondoa vitu katika nyumba hiyo
kabla kuhani hajaingia kuliona
pigo, asije akatangaza kila
kitu kilicho katika nyumba
hiyo kuwa si safi; kisha ku-
hani ataingia na kuiona nyu-
mba hiyo. **37** Atakapokuwa
ameliona pigo hilo, ndipo iki-
wa pigo liko katika kuta za
nyumba hiyo, pamoja na mibo-
nyeo ya rangi ya kijani-manja-
no au ya rangi nyekundu-nye-

SURA 14

a Law 14:17

b Law 14:10
Law 14:18

c Law 12:8
Law 14:22
2Ko 8:12

d Law 5:7

e Law 1:14

f Law 14:20

g Law 23:10
Hes 35:10
Kum 26:1

h Mwa 17:8
Hes 32:22
Kum 6:10

i Kum 7:12
Kum 7:15
Met 3:33

Safu ya 2

a Hes 12:15

b Law 10:10
Law 13:6

c Law 13:56

d Law 14:3
Eze 44:23

e Law 13:51

f Law 14:41

g Law 14:38

h Law 11:24
Law 15:8
Law 17:15
Law 22:6
Hes 19:7

kundu, nayo yaonekana kuwa
imepenya ndani ya uso wa ukuta,
38 ndipo kuhani atatoka
nje ya mlango wa nyumba hiyo
naye ataitenga[a] nyumba hiyo
kwa siku saba.

39 "Naye kuhani atarudi ka-
tika siku ya saba na kutazama;[b]
na ikiwa pigo hilo limeenea
katika kuta za nyumba hiyo,
40 ndipo kuhani atatoa ma-
agizo, nao watayang'oa[c] mawe
ambayo ndani yake mna pigo
hilo, nao watayatupa nje ya
jiji katika mahali pasipo safi.
41 Naye atafanya nyumba hiyo
ikwanguliwe kotekote upande
wa ndani, nao watamwaga sa-
ruji ya udongo ambao wame-
kwangua nje ya jiji katika ma-
hali pasipo safi. **42** Nao wata-
chukua mawe mengine na ku-
yaingiza mahali pa yale mawe
ya zamani; naye atafanya saru-
ji tofauti ya udongo ichukuliwe,
naye atafanya nyumba hiyo ipi-
gwe lipu.

43 "Hata hivyo, ikiwa pigo
hilo litarudi nalo litokee ka-
tika nyumba hiyo baada ya
kuyang'oa mawe hayo na baada
ya kuikwangua nyumba hiyo
na kuipiga lipu, **44** ndipo ku-
hani[d] ataingia ndani na kutaza-
ma; na ikiwa pigo hilo limeenea
katika nyumba hiyo, ni uko-
ma hatari[e] ulio katika nyumba
hiyo. Si safi. **45** Naye atafa-
nya nyumba hiyo ibomolewe
pamoja na mawe yake na mbao
zake na saruji yote ya udongo
ya nyumba hiyo, naye atafa-
nya vichukuliwe nje ya jiji mpa-
ka mahali pasipo safi.[f] **46** La-
kini yeyote atakayeingia ndani
ya nyumba hiyo siku yoyote ya
kutengwa[g] kwake, atakuwa asi-
ye safi mpaka jioni;[h] **47** na ye-
yote anayelala katika nyumba

hiyo atayafua mavazi yake,[a] na yeyote anayekula katika nyumba hiyo atayafua mavazi yake.

48 "Hata hivyo, ikiwa kuhani ataingia na kuangalia, na, tazama sasa, pigo halijaenea katika nyumba baada ya kuipiga lipu nyumba hiyo, basi kuhani ataitangaza nyumba hiyo kuwa safi, kwa sababu pigo hilo limepona.[b] **49** Na ili kuitakasa nyumba hiyo kutokana na dhambi atachukua ndege wawili[c] na mti wa mwerezi[d] na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili[e] na hisopo. **50** Naye atamuua ndege mmoja katika chombo cha udongo juu ya maji yanayotiririka.[f] **51** Naye atauchukua ule mti wa mwerezi na ile hisopo[g] na kile kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kuvichovya katika damu ya yule ndege aliyeuawa juu ya maji yanayotiririka, naye ataitapanya[h] kuelekea nyumba hiyo mara saba.[i] **52** Naye ataitakasa nyumba hiyo kutokana na dhambi kwa damu ya yule ndege na yale maji yanayotiririka na yule ndege aliye hai na ule mti wa mwerezi na ile hisopo na kile kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili. **53** Naye atamwacha yule ndege aliye hai aende zake nje ya jiji mpaka porini naye atafanya upatanisho[j] kwa ajili ya nyumba hiyo; nayo itakuwa safi.

54 "Hiyo ndiyo sheria juu ya pigo la ukoma[k] na juu ya kuanguka kwa nywele kusiko kwa kawaida[l] **55** na juu ya ukoma wa vazi[m] na katika nyumba, **56** na juu ya upele na kigaga na doa,[n] **57** ili kutoa maagizo[o] wakati kitu fulani si safi na wakati kitu fulani ni safi. Hiyo ndiyo sheria juu ya ukoma."[a]

15 Na Yehova akaendelea kusema na Musa na Haruni, na kuwaambia: **2** "Sema na wana wa Israeli, nanyi mtawaambia, 'Ikiwa mwanamume yeyote ana mtiririko unaotoka[b] katika kiungo chake cha uzazi, kile kinachomtoka si safi. **3** Nao huu utakuwa uchafu wake kutokana na kinachomtoka: Iwe kiungo chake cha uzazi kimetiririka kwa mtiririko unaotoka au kiungo chake cha uzazi kimezuiliwa kutokana na mtiririko wake unaotoka, huo ni uchafu wake.

4 "'Kitanda chochote ambacho yule mwenye mtiririko unaotoka atalalia kitakuwa si safi, na chombo chochote ambacho atakalia kitakuwa si safi. **5** Na mtu ambaye atagusa kitanda chake atayafua mavazi yake, naye ataoga katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni.[c] **6** Na yeyote atakayeketi juu ya chombo chochote ambacho yule mwenye mtiririko unaotoka alikuwa amekalia atayafua[d] mavazi yake, naye ataoga katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni. **7** Na yeyote atakayegusa mwili wa mtu mwenye mtiririko unaotoka[e] atayafua mavazi yake, naye ataoga katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni.[f] **8** Na ikiwa mtu mwenye mtiririko unaotoka atamtemea mate mtu aliye safi, ndipo atayafua mavazi yake na kuoga katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni. **9** Na matandiko[g] yoyote ambayo yule mwenye mtiririko unaotoka alikuwa ameyapanda yatakuwa si safi. **10** Na mtu yeyote atakayegusa chochote

SURA 14
a Law 11:25; Law 13:6; Law 15:5; Hes 8:7
b Law 14:3; Kum 32:39
c Law 1:14
d Law 14:4; Hes 19:6
e Ebr 9:19
f Law 14:6
g Kut 12:22; Hes 19:18; 1Fa 4:33; Zb 51:7
h Ebr 9:13; 1Pe 1:2
i Law 14:7
j Law 12:8; Law 14:20; Ebr 2:17
k Law 13:59
l Law 13:30
m Law 13:47
n Law 13:2
o Law 10:10; Eze 44:23

Safu ya 2
a Kum 24:8

SURA 15
b Law 22:4; Hes 5:2; 2Sa 3:29
c Law 11:25; Law 17:15
d Isa 1:16
e Law 22:4; Hes 5:2; 2Sa 3:29
f Law 11:24; Law 17:15
g Mwa 31:34

kilicho chini yake atakuwa asiye safi mpaka jioni; naye atakayevichukua atayafua mavazi yake, naye ataoga katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni. **11** Na mtu yeyote ambaye yule mwenye mtiririko unaotoka[a] atamgusa kabla hajanawa mikono yake katika maji atayafua mavazi yake katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni. **12** Na chombo cha udongo ambacho yule mwenye mtiririko unaotoka atagusa kitavunjwa;[b] na chombo chochote cha mbao[c] kitaoshwa katika maji.

13 "'Sasa, ikiwa yule mwenye mtiririko unaotoka atakuwa safi kutokana na mtiririko wake unaotoka, basi atajihesabia siku saba kwa ajili ya utakaso[d] wake, naye atayafua mavazi yake na kuoga mwili wake katika maji yanayotiririka;[e] naye atakuwa safi. **14** Na katika siku ya nane atajichukulia njiwa-tetere[f] wawili au hua wawili wachanga, naye atakuja mbele za Yehova kwenye mwingilio wa hema la mkutano na kumpa kuhani. **15** Naye kuhani atawatoa, mmoja kuwa toleo la dhambi na yule mwingine kuwa toleo la kuteketezwa;[g] naye kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake mbele za Yehova kuhusiana na mtiririko wake unaotoka.

16 "'Sasa, mwanamume akitokwa na shahawa,[h] basi ataoga mwili wake wote katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni. **17** Na vazi lolote na ngozi yoyote ambazo shahawa iliyotoka itakuwa juu yake zitafuliwa katika maji nazo zitakuwa si safi mpaka jioni.[i]

18 "'Naye mwanamke ambaye mwanamume atalala naye na kutokwa na shahawa, wataoga katika maji na kuwa wasio safi[a] mpaka jioni.

19 "'Na ikiwa mwanamke ana mtiririko unaotoka, nao mtiririko wake unaotoka katika mwili wake uwe ni damu,[b] ataendelea kwa siku saba kuwa katika uchafu[c] wake wa hedhi,[d] na yeyote atakayemgusa atakuwa asiye safi mpaka jioni. **20** Na kitu chochote ambacho atalalia katika uchafu wake wa hedhi kitakuwa si safi,[e] na kila kitu ambacho atakalia kitakuwa si safi. **21** Na mtu yeyote anayegusa kitanda chake atayafua mavazi yake, naye ataoga katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni.[f] **22** Na mtu yeyote atakayegusa chombo chochote alichokuwa akikalia atayafua mavazi yake, naye ataoga katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni.[g] **23** Na ikiwa alikuwa amekalia kitanda au chombo kingine, kwa kukigusa[h] atakuwa asiye safi mpaka jioni. **24** Na ikiwa mwanamume atalala naye na uchafu wake wa hedhi uwe juu yake,[i] ndipo atakuwa asiye safi kwa siku saba, na kitanda chochote ambacho mwanamume huyo huenda akalalia kitakuwa si safi.

25 "'Naye mwanamke, ikiwa mtiririko unaotoka wa damu yake utatiririka kwa siku nyingi[j] wakati ambapo si wakati wa kawaida wa uchafu wake wa hedhi,[k] au ikiwa atakuwa na mtiririko mrefu kuliko uchafu wake wa hedhi, siku zote za mtiririko wake unaotoka usio safi zitakuwa kama siku za uchafu wake wa hedhi. Yeye si safi. **26** Kitanda chochote ambacho huenda atalalia katika yoyote ya siku za mtiri-

SURA 15

a Law 15:2

b Law 6:28
Law 11:33

c Kut 7:19
Law 11:32

d Law 14:8
Law 14:23

e Law 15:5

f Law 1:14
Law 14:22
Hes 6:10

g Law 5:7
Law 14:19
Law 14:31

h Law 22:4
Kum 23:10

i Law 11:25

Safu ya 2

a Kut 19:15
1Sa 21:5

b Law 20:18

c Eze 22:10
Eze 36:17

d Law 12:2
Law 12:5
Law 15:26

e Law 15:4

f Law 15:5

g Law 15:6

h Law 15:10

i Law 18:19
Law 20:18

j Mt 9:20
Mk 5:25
Lu 8:43

k Law 12:2
Law 15:19

riko wake unaotoka kitakuwa kwake kitanda cha uchafu
wa hedhi,[a] na chombo chochote ambacho huenda atakalia ki-
takuwa si safi kama ule uchafu wake wa hedhi. **27** Na mtu
yeyote atakayevigusa[b] atakuwa asiye safi, naye atayafua ma-
vazi yake na kuoga katika maji na kuwa asiye safi mpaka jioni.
28 "'Hata hivyo, ikiwa amekuwa safi kutokana na mtiri-
riko wake unaotoka, atajihesabia pia siku saba, kisha atakuwa safi.[c] **29** Na katika siku ya
nane atajichukulia njiwa-tetere[d] wawili au hua wawili wacha-
nga, naye atawaleta kwa kuhani katika mwingilio wa hema
la mkutano.[e] **30** Naye kuhani atamfanya mmoja kuwa toleo
la dhambi na yule mwingine kuwa toleo la kuteketezwa;[f]
naye kuhani atafanya upatanisho[g] kwa ajili yake mbele
za Yehova kuhusiana na mtiririko wake unaotoka ambao si
safi.
31 "'Nanyi mtawatenga wana wa Israeli kutoka kwa uchafu
wao, wasije wakafa katika uchafu wao kwa kuinajisi maskani
yangu, iliyo katikati yao.[h]
32 "'Hiyo ndiyo sheria juu ya mwanamume aliye na mti-
ririko unaotoka[i] na mwanamume ambaye ametokwa na shaha-
wa[j] na kuwa asiye safi kutokana nayo; **33** na mwanamke aliye
na hedhi[k] katika uchafu wake, na mtu yeyote aliye na
mtiririko wake unaotoka,[l] awe mwanamume au mwanamke,
na awe ni mwanamume anayelala na mwanamke asiye safi.'"

16 Na Yehova akasema na Musa baada ya kifo cha
wana wawili wa Haruni, waliokufa kwa sababu ya kukaribia
kwao mbele za Yehova.[a] **2** Na Yehova akamwambia Musa:
"Sema na Haruni ndugu yako, asiwe akija nyakati zote katika
mahali patakatifu[b] ndani ya pazia,[c] mbele ya kifuniko kilicho
juu ya Sanduku, asije akafa;[d] kwa sababu nitaonekana kati-
ka wingu[e] juu ya kifuniko[f] hicho.
3 "Haruni ataingia pamoja na vitu hivi katika mahali pa-
takatifu:[g] pamoja na ng'ombe-dume mchanga kwa ajili ya to-
leo la dhambi[h] na kondoo-dume kwa ajili ya toleo la kuteketezwa.[i] **4** Anapaswa kuvaa ile
kanzu takatifu ya kitani,[j] nayo ile suruali[k] ya kitani itakuwa
mwilini mwake, naye atajifunga kwa ukumbuu[l] wa kitani
na kujivika kile kilemba[m] cha kitani. Hayo ni mavazi matakatifu.[n] Naye atauosha mwili
wake katika maji[o] na kuyavaa.
5 "Na kutoka katika kusanyiko la wana wa Israeli[p] atachukua wana-mbuzi dume
wawili kwa ajili ya toleo la dhambi[q] na kondoo-dume mmoja
kwa ajili ya toleo la kuteketezwa.[r]
6 "Naye Haruni atamtoa yule ng'ombe-dume wa toleo la
dhambi, aliye kwa ajili yake,[s] naye atafanya upatanisho[t] kwa
ajili yake mwenyewe[u] na nyumba yake.[v]
7 "Naye atawachukua wale mbuzi wawili na kuwasimamisha mbele za Yehova kwenye
mwingilio wa hema la mkutano. **8** Na Haruni atapiga kura[w] juu ya mbuzi hao wawi-
li, kura moja kwa ajili ya Yehova na ile nyingine kwa ajili ya Azazeli.[x] **9** Naye Haruni atamtoa yule mbuzi ambaye
kura[y] ilimwangukia kwa ajili ya

SURA 15
a Law 15:21
b Law 15:10
Law 15:22
c Law 15:13
d Law 1:14
Law 15:14
e Hes 6:10
f Law 5:7
Law 14:31
Law 15:15
g Law 4:31
Law 12:7
1Yo 2:2
h Law 19:30
Hes 5:3
Hes 19:20
i Law 15:2
j Law 15:16
k Law 15:19
l Law 15:25

Safu ya 2

SURA 16
a Law 10:2
b Kut 30:10
Law 23:27
Ebr 9:7
c Kut 40:21
Ebr 6:19
Ebr 9:3
Ebr 10:20
d Hes 4:19
e Kut 40:34
f Kut 25:22
g Kut 26:33
Ebr 9:7
h Law 4:3
i Law 1:3
Law 8:18
j Kut 28:39
Ufu 19:8
k Kut 28:42
l Kut 39:29
m Kut 28:4
1Ko 11:3
n Kut 28:2
o Kut 30:20
Ebr 10:22
p Law 4:14
Ebr 7:27
q Hes 29:11
2Nya 29:21
Ezr 6:17
r Law 1:3
s Law 8:14
Ebr 9:7
t Ebr 10:1
u Law 9:7
Ebr 5:3
v Kut 30:30
Zb 135:19
w Hes 26:55
Yos 18:10
x Law 14:7
Law 14:53
y Met 16:33

Yehova, naye atamfanya kuwa toleo la dhambi.[a] **10** Lakini yule mbuzi aliyeangukiwa na kura kwa ajili ya Azazeli atasimamishwa akiwa hai mbele za Yehova ili kufanya upatanisho kwa ajili yake, ili kumpeleka[b] nyikani[c] kwa ajili ya Azazeli.

11 "Na Haruni atamtoa yule ng'ombe-dume wa toleo la dhambi, aliye kwa ajili yake, na kufanya upatanisho kwa ajili yake mwenyewe na nyumba yake; naye atamchinja ng'ombe-dume huyo wa toleo la dhambi, aliye kwa ajili yake.[d]

12 "Naye atachukua chetezo[e] kilichojaa makaa yanayowaka moto kutoka katika madhabahu[f] mbele za Yehova, na mikono yake yote miwili[g] ikiwa imejaa uvumba uliotiwa manukato,[h] naye atavileta ndani ya pazia.[i] **13** Pia atautia uvumba juu ya moto mbele za Yehova,[j] nalo wingu la uvumba litafunika kifuniko cha Sanduku,[k] kilicho juu ya ule Ushuhuda,[l] asije akafa.

14 "Naye atachukua sehemu ya damu ya ng'ombe-dume[m] na kuitapanya kwa kidole chake mbele ya kifuniko upande wa mashariki, naye atatapanya[n] sehemu ya damu hiyo kwa kidole chake mara saba mbele ya kifuniko.[o]

15 "Naye atamchinja yule mbuzi wa toleo la dhambi, aliye kwa ajili ya watu,[p] naye ataileta damu yake ndani ya pazia[q] na kufanya na hiyo damu[r] sawa na vile alivyofanya na ile damu ya ng'ombe-dume; naye ataitapanya kukielekea kifuniko na mbele ya kifuniko.

16 "Naye atafanya upatanisho kwa ajili ya mahali patakatifu kuhusiana na uchafu[s] wa wana wa Israeli na kuhusiana na maasi yao katika dhambi zao zote;[a] na hivyo ndivyo anavyopaswa kufanya kwa ajili ya hema la mkutano, linalokaa pamoja nao katikati ya uchafu wao.

17 "Na mtu mwingine yeyote asiwemo katika hema la mkutano tangu anapoingia ndani ili kufanya upatanisho mpaka atakapotoka nje; naye atafanya upatanisho kwa ajili yake mwenyewe[b] na kwa ajili ya nyumba yake na kwa ajili ya kutaniko lote la wana wa Israeli.[c]

18 "Naye atatoka nje kwenda kwenye madhabahu,[d] iliyo mbele za Yehova, na kufanya upatanisho kwa ajili yake, naye atachukua sehemu ya damu ya yule ng'ombe-dume na sehemu ya damu ya yule mbuzi na kuitia juu ya pembe za ile madhabahu kuizunguka pande zote.[e] **19** Pia atatapanya[f] sehemu ya damu juu yake kwa kidole chake mara saba na kuisafisha na kuitakasa kutokana na uchafu wa wana wa Israeli.

20 "Atakapokuwa amemaliza kufanya upatanisho[g] kwa ajili ya mahali patakatifu na lile hema la mkutano na ile madhabahu, atamtoa pia yule mbuzi aliye hai.[h] **21** Na Haruni ataweka mikono yake miwili[i] juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai na kuungama[j] juu yake makosa[k] yote ya wana wa Israeli na maasi yao yote na dhambi[l] zao zote, naye atayaweka juu ya kichwa cha yule mbuzi[m] na kumpeleka mpaka nyikani[n] kwa mkono wa mtu aliye tayari.[o] **22** Naye mbuzi huyo atachukua juu yake mwenyewe

SURA 16

a Mdo 2:23
b Law 14:7
c Law 16:22; Isa 53:4; Ro 15:3
d Law 16:6
e Ebr 9:4
f Kut 40:29; Law 6:13; Hes 16:46
g Ufu 8:4
h Kut 30:34; Kut 30:36; Mdo 10:4; Ufu 5:8; Ufu 8:3
i Law 16:2; Ebr 6:19; Ebr 10:20
j Kut 25:22; Hes 16:7; 2Fa 19:15
k Kut 25:18; Kut 25:21; 1Nya 28:11
l Kut 25:21; Kut 34:29
m Ebr 9:22
n Ebr 9:12; 1Pe 1:2
o Ro 3:25; Ebr 9:24; Ebr 9:25; Ebr 10:4; Ebr 10:12
p Law 16:5; Ebr 2:17; Ebr 5:3; Ebr 9:26; 1Yo 2:1; 1Yo 2:2
q Ebr 6:19; Ebr 9:3; Ebr 9:7; Ebr 10:20
r Law 17:11; Ebr 9:22
s Zb 51:5; Mhu 7:20; Ro 3:23

Safu ya 2

a Kum 32:5; 1Fa 8:46
b Law 9:7; Law 16:6; Ebr 7:27
c Isa 53:6; Mk 10:45; Ebr 2:9; Ebr 9:7; Ebr 9:12; 1Yo 2:2; Ufu 1:5
d Kut 38:1; Law 16:12
e Law 9:9; Ebr 9:22
f Law 9:12
g Kut 29:36; Law 8:15; Law 16:16; Ebr 9:23
h Law 16:8; Law 16:10; Ufu 5:9
i Law 1:4
j Ne 1:6
k Zb 69:9; Isa 53:5; Efe 2:3
l 1Ko 15:3; 1Pe 2:24
m Isa 53:6; 2Ko 5:21
n Law 14:7

o Mt 4:1; Lu 4:1.

makosa[a] yao yote mpaka katika
nchi ya jangwa,[b] naye atampe-
leka mbuzi huyo nyikani.[c]
23 "Naye Haruni ataingia
katika hema la mkutano na ku-
vua yale mavazi ya kitani aliyo-
kuwa amevaa alipoingia maha-
li patakatifu, naye atayaweka
hapo chini.[d] **24** Naye ataoga
mwili wake katika maji[e] kati-
ka mahali patakatifu[f] na ku-
vaa mavazi[g] yake na kutoka
nje na kutoa toleo lake la kute-
ketezwa[h] na toleo la kuteketez-
wa la watu[i] na kufanya upata-
nisho kwa ajili yake mwenyewe
na kwa ajili ya watu.[j] **25** Naye
atayafukiza mafuta ya toleo la
dhambi juu ya madhabahu.[k]
26 "Na yule[l] aliyempeleka
yule mbuzi kwa ajili ya Aza-
zeli,[m] atayafua mavazi yake,
naye ataoga mwili wake katika
maji,[n] kisha anaweza kuingia
kambini.
27 "Hata hivyo, yule ng'o-
mbe-dume wa toleo la dhambi
na yule mbuzi wa toleo la dha-
mbi, ambao damu yao ililetwa
ndani ili kufanya upatanisho,
atawapeleka mpaka nje ya ka-
mbi; nao watateketeza ngozi
zao na nyama yao na mavi yao
katika moto.[o] **28** Na yule ali-
yewateketeza atayafua mavazi
yake, naye ataoga mwili wake
katika maji, kisha anaweza ku-
ingia kambini.
29 "Na itakuwa sheria mpa-
ka wakati usio na kipimo kwe-
nu ninyi:[p] Katika mwezi wa
saba, siku ya kumi ya mwezi
huo,[q] mtazitesa nafsi zenu,[r] na-
nyi msifanye kazi yoyote,[s] iwe
ni mwenyeji au mkaaji mgeni
anayekaa akiwa mgeni katika-
ti yenu. **30** Kwa maana kati-
ka siku hii upatanisho[t] utafa-
nywa kwa ajili yenu ili kuwata-

SURA 16
a Isa 53:12 Yoh 1:29 Ro 15:3 Efe 1:7 Ebr 9:28 1Pe 2:24 1Yo 3:5
b Zb 103:12 Eze 18:22 Mik 7:19 Ebr 13:12
c Law 16:10
d Eze 42:14 Eze 44:19
e Kut 30:20 Ebr 9:9 Ebr 10:22
f Law 6:16 Law 6:26
g Kut 28:4 Law 8:7
h Law 16:3
i Law 16:5
j Efe 1:7
k Kut 29:13 Law 3:16
l Law 16:21
m Law 16:8
n Hes 19:7 Ebr 9:10
o Law 4:12 Law 8:17 Ebr 13:11 Ebr 13:12
p Kut 30:10
q Law 23:27 Hes 29:7
r Zb 35:13 Isa 58:5 2Ko 7:10
s Law 23:28
t Yoh 3:16 Ro 8:32 Tit 2:14 1Yo 1:7 1Yo 3:16

Safu ya 2
a Zb 51:2 Yer 33:8 Eze 36:25 Efe 5:26 Ebr 9:14 Ebr 10:2
b Law 23:32
c Kut 29:7 Law 8:12 Mdo 10:38 Ebr 1:9
d Kut 29:29 Law 8:33 Ebr 5:5 Ebr 5:10 Ebr 7:11 Ebr 7:16
e Hes 20:26
f Kut 28:39 Kut 39:28 Law 16:4
g Kut 28:2 Ufu 19:8
h Law 16:16
i Law 16:20
j Kut 29:36 Law 8:15 Law 16:18
k Law 16:24 1Yo 2:2
l Law 23:31 Hes 29:7
m Kut 30:10 Ebr 9:7

ngaza kuwa safi. Mtakuwa safi
kutokana na dhambi zenu zote
mbele za Yehova.[a] **31** Ni saba-
to[b] ya pumziko kamili kwenu,
nanyi mtazitesa nafsi zenu. Ni
sheria mpaka wakati usio na ki-
pimo.
32 "Naye kuhani atakayeti-
wa mafuta[c] na ambaye mko-
no wake utajazwa nguvu ili ku-
tenda akiwa kuhani,[d] ataka-
yemfuata[e] baba yake, atafa-
nya upatanisho naye atavaa
yale mavazi ya kitani.[f] Hayo ni
mavazi matakatifu.[g] **33** Naye
atafanya upatanisho kwa ajili
ya patakatifu zaidi,[h] na kwa aji-
li ya hema[i] la mkutano na kwa
ajili ya madhabahu[j] atafanya
upatanisho; na kwa ajili ya ma-
kuhani na kwa ajili ya watu
wote wa kutaniko atafanya
upatanisho.[k] **34** Na hiyo ita-
kuwa sheria kwenu mpaka wa-
kati usio na kipimo,[l] ili ku-
fanya upatanisho kwa ajili ya
wana wa Israeli kuhusu dhambi
zao zote mara moja kwa mwa-
ka."[m]
Basi akafanya kama vile Ye-
hova alivyokuwa amemwamu-
ru Musa.

17 Na Yehova akaendelea
kusema na Musa, na ku-
mwambia: **2** "Sema na Haru-
ni na wanawe na wana wote
wa Israeli, nawe uwaambie,
'Hili ndilo jambo ambalo Yeho-
va ameamuru, na kusema:
3 ""Mtu yeyote wa nyumba
ya Israeli atakayemchinja ng'o-
mbe-dume au mwana-kondoo
dume au mbuzi katika kambi
au atakayemchinja nje ya ka-
mbi **4** naye asimlete kwenye
mwingilio wa hema la mku-
tano[n] ili kumtoa awe toleo kwa

SURA 17 n Law 1:3; Kum 6:1; Kum 12:21.

Yehova mbele ya maskani ya
Yehova, mtu huyo atahesabiwa
kuwa na hatia ya damu. Amemwaga damu, naye mtu huyo
lazima akatiliwe mbali kutoka
katikati ya watu wake,[a] **5** ili
kwamba wana wa Israeli walete
dhabihu zao, wanazozitoa dhabihu katika uwanja,[b] nao wata-
zileta kwa Yehova kwenye mwingilio wa hema la mkutano kwa
kuhani,[c] nao watatoa dhabihu
hizo zikiwa dhabihu za ushirika kwa Yehova.[d] **6** Naye ku-
hani atainyunyiza damu juu ya
madhabahu[e] ya Yehova kwenye mwingilio wa hema la mku-
tano, naye atayafukiza mafuta[f] yawe harufu ya kumtuliza
Yehova.[g] **7** Kwa hiyo hawa-
paswi tena kutoa dhabihu zao
kwa wale roho waovu wenye
umbo la mbuzi[h] wanaofanya ua-
sherati[i] pamoja nao. Hiyo ita-
kuwa sheria kwenu mpaka wa-
kati usio na kipimo, katika vi-
zazi vyenu vyote."'

8 "Nawe utawaambia, 'Mtu
yeyote wa nyumba ya Israeli
au mkaaji mgeni yeyote amba-
ye huenda akawa anakaa aki-
wa mgeni katikati yenu ana-
yetoa toleo la kuteketezwa[j]
au dhabihu **9** naye asiilete
kwenye mwingilio wa hema la
mkutano ili kuitoa kwa Yeho-
va,[k] mtu huyo lazima akatiliwe
mbali kutoka kwa watu wake.[l]

10 "'Na mtu yeyote wa nyu-
mba ya Israeli au mkaaji mgeni
yeyote anayekaa akiwa mgeni
katikati yenu atakayekula na-
mna yoyote ya damu,[m] nitauwe-
ka uso wangu dhidi ya nafsi[n]
hiyo inayokula damu, nami ha-
kika nitamkatilia mbali ku-
toka katikati ya watu wake.
11 Kwa maana nafsi ya mwi-
li iko katika damu,[o] nami mwe-
nyewe nimeiweka juu ya ma-
dhabahu ili ninyi mfanye upa-
tanisho[a] kwa ajili ya nafsi zenu,
kwa sababu damu[b] ndiyo hufa-
nya upatanisho[c] kupitia nafsi
iliyo ndani yake. **12** Ndiyo sa-
babu nimewaambia wana wa
Israeli: "Nafsi yoyote kati yenu
isile damu na mkaaji mgeni
yeyote anayekaa akiwa mge-
ni katikati yenu[d] hapaswi kula
damu."[e]

13 "'Na mtu yeyote kati ya
wana wa Israeli au mkaaji mge-
ni yeyote anayekaa akiwa mge-
ni katikati yenu ambaye katika
kuwinda anamkamata mnya-
ma-mwitu au ndege anayeweza
kuliwa, basi ataimwaga damu[f]
yake na kuifunika kwa mavu-
mbi.[g] **14** Kwa maana nafsi ya
kila namna ya mwili ni damu
yake kwa nafsi iliyo ndani yake.
Basi niliwaambia wana wa Isra-
eli: "Hamtakula damu ya mwili
wa namna yoyote, kwa sababu
nafsi ya kila mwili wa namna
yoyote iko katika damu yake.[h]
Mtu yeyote atakayeila atakati-
liwa mbali."[i] **15** Nayo nafsi
yoyote itakayokula mwili ulio-
kufa tayari au kitu kilichoraru-
liwa na mnyama-mwitu,[j] awe ni
mwenyeji au mkaaji mgeni, basi
atayafua mavazi yake na kuo-
ga katika maji na kuwa asiye
safi[k] mpaka jioni; naye atakuwa
safi. **16** Lakini ikiwa hataya-
fua naye hataoga mwili wake,
basi atajibu kwa kosa lake.'"[l]

18 Na Yehova akaendelea
kusema na Musa, na ku-
mwambia: **2** "Sema na wana
wa Israeli, nawe utawaambia,
'Mimi ni Yehova Mungu wenu.[m]
3 Jinsi inavyofanya nchi ya Mi-
sri ambamo mlikaa, msifanye;[n]
na jinsi inavyofanya nchi ya
Kanaani, ambamo nitawaleta,

SURA 17
a Law 18:29; Law 20:2
b 2Fa 16:4; Eze 20:28
c Kum 12:5; Kum 12:18
d Law 3:2; Law 7:11
e Law 3:8
f Law 3:16; Law 7:31
g Law 3:5; Law 4:31
h Kum 32:17; Yos 24:14; 2Nya 11:15; 1Ko 10:20
i Kut 34:15; Law 20:5; Kum 31:16; Yer 3:1; Eze 23:8; Yak 4:4
j Law 1:3
k Kum 12:6; Kum 12:14
l Law 17:4
m Mwa 9:4; Law 3:17; Law 7:26; Law 19:26; Kum 12:16; 1Sa 14:33; Mdo 15:29
n Law 20:3; Zb 34:16; Yer 44:11; 1Pe 3:12
o Mwa 9:4; Law 17:14; Kum 12:23; 1Nya 11:19

Safu ya 2
a Law 8:15; Law 16:18
b Mt 26:28; Mk 14:24; Ro 3:25; Ro 5:9; Efe 1:7; Kol 1:20
c Ebr 9:22; Ebr 13:12; 1Pe 1:2; 1Yo 1:7; Ufu 1:5
d Kut 12:49
e Mwa 9:4; Kum 12:23; 1Nya 11:19; Mdo 15:20; Mdo 15:29
f Kum 12:16; Kum 15:23
g Eze 24:7
h Law 17:11; Kum 12:23
i Law 17:10
j Kut 22:31; Kum 14:21
k Law 11:40
l Law 7:18; Hes 19:20

SURA 18
m Mwa 17:7; Kut 6:7; Law 11:44; Mk 12:29
n Zb 106:35; Eze 20:7; Yak 4:4

msifanye;[a] na katika sheria zao
msitembee. **4** Maamuzi ya-
ngu ya hukumu[b] mtayatenda,
na sheria[c] zangu mtazishika ili
kutembea katika hizo.[d] Mimi ni
Yehova Mungu wenu. **5** Na-
nyi mtazishika sheria zangu na
maamuzi yangu ya hukumu,
ambazo ikiwa mtu atazifanya,
yeye pia ataishi kwa hizo.[e] Mimi
ni Yehova.[f]
6 "'Yeyote kati yenu asimka-
ribie mtu yeyote wa jamaa
yake, wa kimwili, wa karibu ili
kufunua uchi.[g] Mimi ni Yehova.
7 Uchi wa baba yako[h] na uchi
wa mama yako usiufunue. Yeye
ni mama yako. Usiufunue uchi
wake.
8 "'Uchi wa mke wa baba
yako usiufunue.[i] Ni uchi wa
baba yako.
9 "'Nao uchi wa dada yako,
binti ya baba yako au binti ya
mama yako, awe amezaliwa ka-
tika nyumba hiyo hiyo au ame-
zaliwa nje, usiufunue uchi wao.[j]
10 "'Nao uchi wa binti ya
mwana wako au binti ya binti
yako, usiufunue uchi wao, kwa
sababu wao ni uchi wako.
11 "'Nao uchi wa binti ya
mke wa baba yako, uzao
wa baba yako, kwa kuwa yeye
ni dada yako, usiufunue uchi
wake.
12 "'Uchi wa dada ya baba
yako usiufunue. Yeye ana uhu-
siano wa damu na baba yako.[k]
13 "'Uchi wa dada ya mama
yako usiufunue, kwa sababu
yeye ana uhusiano wa damu na
mama yako.
14 "'Uchi wa ndugu ya baba
yako usiufunue. Usimkaribie
mke wake. Yeye ni shangazi
yako.[l]
15 "'Uchi wa binti-mkwe[m]
wako usiufunue. Yeye ni mke
wa mwana wako. Usiufunue
uchi wake.
16 "'Uchi wa mke wa ndu-
gu yako[a] usiufunue. Ni uchi wa
ndugu yako.
17 "'Uchi wa mwanamke na
binti yake usiufunue.[b] Binti ya
mwana wake na binti ya binti
yake usimchukue ili kuufunua
uchi wake. Wao wana uhusiano
wa damu. Ni mwenendo mpo-
tovu.[c]
18 "'Nawe usimchukue mwa-
namke pamoja na dada yake
awe mshindani[d] ili kuufunua
uchi wake, yaani, pamoja naye
akiwa angali hai.
19 "'Nawe usimkaribie mwa-
namke wakati wa hedhi[e] ya
uchafu wake ili kuufunua uchi
wake.[f]
20 "'Nawe usimpe mke wa
mwenzako shahawa inayoku-
toka awe asiye safi kutokana
nayo.[g]
21 "'Nawe usiuruhusu uzao
wako wowote utolewe[h] kwa Mo-
leki.[i] Usilitie unajisi[j] jina la Mu-
ngu wako kwa njia hiyo. Mimi
ni Yehova.[k]
22 "'Nawe usilale na mwana-
mume[l] kama vile unavyolala na
mwanamke.[m] Ni jambo lenye
kuchukiza.
23 "'Nawe usimpe mnyama
yeyote shahawa[n] yako awe asi-
ye safi kutokana nayo, na mwa-
namke asisimame mbele ya
mnyama ili kuungana naye.[o] Ni
kuvunja jambo lililo la asili.
24 "'Msijifanye wenyewe
kuwa wasio safi kwa lolote la
mambo hayo, kwa sababu
kwa mambo yote hayo mataifa
ninayoyafukuza kutoka
mbele yenu yamejifanya ye-
nyewe kuwa si safi.[p] **25** Kwa
hiyo nchi si safi, nami nitale-
ta adhabu kwa ajili ya kosa

SURA 18
a Kut 23:24
Law 20:23
Kum 12:30
Yer 10:2
b Law 19:37
Law 20:22
Kum 4:1
c Kum 6:2
Zb 119:16
Eze 20:19
1Yo 5:3
d Lu 1:6
e Eze 20:11
Lu 10:28
Ro 10:5
Ga 3:12
f Kut 6:2
Mal 3:6
g Law 20:17
Ga 5:19
h Mwa 9:22
Eze 22:10
i Mwa 35:22
Law 20:11
Kum 22:30
Kum 27:20
2Sa 16:21
1Ko 5:1
j Law 20:17
Kum 27:22
2Sa 13:12
Eze 22:11
k Law 20:19
l Law 20:20
m Mwa 38:26
Law 20:12
Eze 22:11

Safu ya 2
a Law 20:21
Kum 25:5
Mk 6:17
Mk 12:19
b Law 20:14
Kum 27:23
c Ga 5:19
d Mwa 30:15
1Sa 1:6
e Law 20:18
f Law 15:19
Law 15:24
Law 20:18
Eze 22:10
g Kut 20:14
Law 20:10
Kum 22:22
2Sa 11:4
Met 6:29
Mt 5:27
1Ko 6:9
Ebr 13:4
h Kum 18:10
i Law 20:2
1Fa 11:7
2Fa 23:10
Mdo 7:43
j Kut 20:7
Law 19:12
Law 20:3
Eze 36:20
k Isa 42:8
l 1Ko 6:9
1Ti 1:10
Yud 7
m Mwa 19:5
Law 20:13
Amu 19:22
Ro 1:27
n Kut 22:19
Law 20:15
o Law 20:16
p Law 20:23
Kum 18:12

lake juu yake, nayo nchi itawatapika wakaaji wake.[a] **26** Nanyi mtazishika sheria zangu na maamuzi yangu ya hukumu,[b] nanyi msifanye lolote la mambo hayo yenye kuchukiza, iwe ni mwenyeji au mkaaji mgeni anayekaa akiwa mgeni katikati yenu.[c] **27** Kwa maana mambo yote hayo yenye kuchukiza, watu wa nchi waliokuwa mbele yenu wameyafanya,[d] hivi kwamba nchi si safi. **28** Ndipo nchi haitawatapika ninyi kwa sababu ya kuitia kwenu unajisi kama vile itakavyoyatapika mataifa yaliyokuwa mbele yenu.[e] **29** Ikiwa mtu yeyote atafanya lolote la mambo yote hayo yenye kuchukiza, basi nafsi zinazoyafanya zitakatiliwa mbali kutoka katikati ya watu wao.[f] **30** Nanyi mtatimiza wajibu wenu kwangu ili kutoendeleza yoyote kati ya desturi hizo zenye kuchukiza ambazo zimeendelezwa mbele yenu,[g] ili msijifanye kuwa wasio safi kutokana nazo. Mimi ni Yehova Mungu wenu.'"

19 Na Yehova akazidi kusema na Musa, na kumwambia: **2** "Sema na kusanyiko lote la wana wa Israeli, nawe utawaambia, 'Muwe watakatifu,[h] kwa sababu mimi Yehova Mungu wenu ni mtakatifu.[i]

3 "'Kila mmoja wenu anapaswa kumwogopa mama yake na baba yake,[j] nazo sabato zangu mnapaswa kuzishika.[k] Mimi ni Yehova Mungu wenu. **4** Msigeukie miungu isiyo na thamani,[l] wala msijifanyie miungu ya kuyeyushwa.[m] Mimi ni Yehova Mungu wenu.

5 "'Sasa ikiwa mtamtolea Yehova dhabihu ya ushirika,[n] mtaitoa ili mjipatie kibali.[a] **6** Inapaswa kuliwa siku ile mnayotoa dhabihu na kesho yake, lakini kitakachobaki mpaka siku ya tatu kitateketezwa kwa moto.[b] **7** Hata hivyo, ikiwa kwa vyovyote kitaliwa siku ya tatu, ni kitu kichafu.[c] Hakitapokewa kwa kibali.[d] **8** Naye atakayekila atajibu kwa kosa lake,[e] kwa sababu amekitia unajisi kitu kitakatifu cha Yehova; nayo nafsi hiyo itakatiliwa mbali kutoka kwa watu wake.

9 "'Na mnapovuna mavuno ya nchi yenu, msivune kabisa ukingo wa shamba lenu, nayo masalio ya mavuno yenu msiyaokote.[f] **10** Pia, usikusanye masalio[g] ya shamba lako la mizabibu, wala usiokote zabibu zilizotawanyika za shamba lako la mizabibu. Ziache kwa ajili ya mwenye kuteseka na mkaaji mgeni.[h] Mimi ni Yehova Mungu wenu.

11 "'Msiibe,[i] wala msidanganye,[j] wala msitendeane kwa uwongo mtu yeyote na mwenzake.[k] **12** Na msiape uwongo kwa jina langu,[l] ili msilitie unajisi jina la Mungu wenu. Mimi ni Yehova. **13** Usimpunje[m] mwenzako, wala usinyang'anye.[n] Usikae na mshahara wa mfanyakazi wa kukodiwa usiku kucha mpaka asubuhi.[o]

14 "'Usimlaani kiziwi, na mbele ya kipofu usiweke kikwazo;[p] nawe umwogope Mungu wako.[q] Mimi ni Yehova.

15 "'Msifanye ukosefu wa haki katika hukumu. Usiwatendee watu wa hali ya chini kwa njia ya ubaguzi,[r] wala usimpendelee mtu mkuu.[s] Utamhukumu mwenzako kwa haki.

SURA 18

a Mwa 15:16
b Law 20:22 Kum 4:1 Kum 4:40 Ro 2:12
c Kut 12:49
d Kum 20:18 2Fa 16:3 2Fa 21:2
e Law 20:22
f Law 20:15
g Law 18:3 Law 20:23 Kum 18:9

SURA 19

h Law 11:44 Efe 1:4 1Pe 1:16
i Law 21:8 Isa 6:3 Ufu 4:8
j Kut 20:12 Efe 6:2 Ebr 12:9
k Kut 20:8 Kut 20:11 Kut 31:13 Lu 6:5
l Kut 20:4 Law 26:1 Zb 96:5 Hab 2:18 1Ko 10:14
m Kut 20:23 Kut 32:4 Kum 27:15
n Law 3:1

Safu ya 2

a Law 7:12
b Law 7:17
c Eze 4:14
d Law 7:18
e Law 5:17
f Kut 23:11 Law 23:22 Kum 24:19
g Isa 17:6 Yer 49:9
h Law 23:6 Kum 15:7 Ru 2:15 Zb 140:12
i Kut 20:15 Efe 4:28
j Law 6:2 Met 12:22 Efe 4:25
k 1Fa 13:18 Yer 9:5
l Kut 20:7 Kum 5:11 Mt 5:37 Yak 5:12
m Met 22:16 Mk 10:19
n Met 22:22
o Kum 24:15 Yer 22:13 Yak 5:4
p Kum 27:18
q Mwa 42:18 Law 25:17 Ne 5:15 Met 1:7 Met 8:13 1Pe 2:17

r Kut 23:3; Kum 16:19; 2Nya 19:6; Met 24:23; Ro 2:11; s Kum 1:17; Yak 2:9.

16 "'Usizunguke katikati ya
watu wako ili kuchongea.[a] Usi-
simame dhidi ya damu ya mwe-
nzako.[b] Mimi ni Yehova.
17 "'Usimchukie ndugu yako
moyoni mwako.[c] Lazima umka-
ripie mwenzako,[d] usije ukachu-
kua dhambi pamoja naye.
18 "'Usilipize kisasi[e] wala
usiwe na kinyongo juu ya wana
wa watu wako;[f] nawe mpende
mwenzako kama wewe mwe-
nyewe.[g] Mimi ni Yehova.
19 "'Mtazishika sheria za-
ngu: Usiwafanye wanyama
wako wa kufugwa wa aina mbi-
li wazaane. Usilipande shamba
lako aina mbili za mbegu,[h] nawe
usivae vazi la aina mbili za nyu-
zi, zilizochanganywa.[i]
20 "'Sasa mwanamume aki-
lala na mwanamke na sha-
hawa imtoke, wakati amba-
po yeye ni mjakazi aliywe-
kwa kwa ajili ya mwanamume
mwingine, naye hajakombole-
wa kwa njia yoyote wala haja-
pewa uhuru, adhabu itatolewa.
Watu hao wasiuawe, kwa sa-
babu hakuwa amewekwa huru.
21 Naye atamletea Yehova to-
leo lake la hatia kwenye mwi-
ngilio wa hema la mkutano, ko-
ndoo-dume wa toleo la hatia.[j]
22 Naye kuhani atafanya upa-
tanisho kwa ajili yake kwa yule
kondoo-dume wa toleo la ha-
tia mbele za Yehova kwa ajili
ya dhambi yake ambayo alite-
nda; naye atasamehewa dhambi
yake ambayo alitenda.[k]
23 "'Na ikiwa mnaingia kati-
ka nchi, na kuupanda mti wo-
wote kwa ajili ya chakula, mta-
yaona matunda yake kuwa ma-
chafu kama "govi" lake. Kwa
miaka mitatu utakuwa hau-
jatahiriwa kwenu. Hayatali-
wa. **24** Lakini katika mwaka
wa nne matunda[a] yake yote ya-
takuwa kitu kitakatifu cha
kusherehekea kwa kushangi-
lia kwa Yehova.[b] **25** Na ka-
tika mwaka wa tano mnaweza
kula matunda yake ili kujionge-
zea mazao yake.[c] Mimi ni Yeho-
va Mungu wenu.
26 "'Msile kitu chochote pa-
moja na damu.[d]
"'Msitafute ishara za bahati,[e]
wala msifanye uchawi.[f]
27 "'Msikate ndevu zenu
ziwe fupi kuzunguka pande
zote, wala usiharibu ncha ya
ndevu zako.[g]
28 "'Na msijikatekate mwili
wenu kwa ajili ya nafsi iliyoku-
fa,[h] wala msijitie alama ya cha-
njo. Mimi ni Yehova.
29 "'Usimtie unajisi binti
yako kwa kumfanya kahaba,[i] ili
nchi isifanye ukahaba na hivyo
nchi ijae maadili mapotovu.[j]
30 "'Sabato zangu mtazishi-
ka,[k] nanyi mtapaheshimu pata-
katifu pangu.[l] Mimi ni Yehova.
31 "'Msiwaendee wenye ku-
wasiliana na pepo,[m] wala msita-
fute shauri la wajuzi wa kuba-
shiri matukio,[n] ili kutiwa unaji-
si nao. Mimi ni Yehova Mungu
wenu.
32 "'Unapaswa kusimama
mbele ya mtu mwenye mvi,[o]
nawe umwonyeshe ufikirio mtu
mzee,[p] nawe umwogope Mungu
wako.[q] Mimi ni Yehova.
33 "'Na ikiwa mkaaji mge-
ni anakaa pamoja nawe aki-
wa mgeni katika nchi yenu,
msimtendee vibaya.[r] **34** Yule
mkaaji mgeni anayekaa aki-
wa mgeni pamoja nanyi ata-
kuwa kwenu kama mwenyeji
wenu; nawe utampenda kama
wewe mwenyewe,[s] kwa maana

SURA 19
a Zb 15:3; Met 11:13; 1Ti 3:11; 2Ti 3:3; Tit 2:3
b Kut 20:16; 1Fa 21:13; Met 6:17; Mt 26:60; Mdo 6:11
c Mwa 27:41; Met 10:18; 1Yo 2:9; 1Yo 3:15
d Zb 141:5; Met 9:8; Mt 18:15; Ga 2:11; 1Ti 5:20; Tit 1:13
e Met 20:22; Ro 12:19
f 1Sa 18:29; Zb 55:3
g Mt 5:43; Mt 22:39; Ro 13:9; Ga 5:14; Yak 2:8
h Kum 22:9
i Kum 22:11
j Law 6:6
k Law 4:31; Law 6:7

Safu ya 2
a Hes 18:12; Kum 18:4
b Kum 26:2; Met 3:9
c Law 26:4
d Law 3:17; Law 17:13; Kum 12:23; Mdo 15:20; Mdo 21:25
e 2Fa 17:17
f Kut 8:7; Kum 18:10; 2Fa 21:6; Ga 5:20; Ufu 21:8
g Law 21:5; Yer 9:26
h Kum 14:1; Yer 16:6
i Law 21:7; Kum 23:17; Ebr 13:4
j Met 21:27; 1Pe 4:3
k Kut 20:10; Kut 31:13
l Law 26:2
m Law 20:6; Kum 18:11; 1Sa 28:7; 1Nya 10:13; 2Nya 33:6; Isa 8:19; Ga 5:20; Ufu 21:8
n Law 20:27; Mdo 16:16
o Met 16:31; Met 20:29
p Ayu 32:6; Met 23:22; Omb 5:12; 1Ti 5:1
q Ne 5:9; Ayu 28:28; Met 1:7; Met 8:13; 1Pe 2:17;
r Kut 23:9; Mal 3:5; s Kut 12:49; Kum 10:19.

mlikuwa wakaaji wageni katika
nchi ya Misri.[a] Mimi ni Yehova
Mungu wenu.
35 "'Msikose kufanya haki
katika kuhukumu,[b] katika ku-
pima, katika kupima uzito[c] au
katika kupima vitu vya maji-
maji. **36** Mtakuwa na mizani
sahihi, vipimo sahihi,[d] kipimo
sahihi cha efa na kipimo sa-
hihi cha hini. Mimi ni Yehova
Mungu wenu, ambaye nimewa-
toa ninyi katika nchi ya Misri.
37 Kwa hiyo mtazishika sheria
zangu zote na maamuzi yangu
yote ya hukumu, nanyi mtazi-
fanya.[e] Mimi ni Yehova.'"

20 Na Yehova akaendelea
kusema na Musa, na ku-
mwambia: **2** "Utawaambia
wana wa Israeli, 'Mtu yeyote wa
wana wa Israeli, na mkaaji mge-
ni yeyote anayekaa akiwa mge-
ni katika Israeli, anayempa Mo-
leki[f] yeyote kati ya uzao wake,
lazima auawe. Watu wa nchi
watampiga kwa mawe mpaka
afe. **3** Mimi nami, nitauweka
uso wangu juu ya mtu huyo,
nami nitamkatilia mbali kuto-
ka katikati ya watu wake,[g] kwa
sababu amempa Moleki baadhi
ya uzao wake kwa kusudi la ku-
patia unajisi mahali pangu pa-
takatifu[h] na kulitia unajisi jina
langu takatifu.[i] **4** Na ikiwa
watu wa nchi hiyo hawatamu-
ua kwa kuyaficha macho yao
kimakusudi yasimwone mtu
huyo anapompa Moleki yeyo-
te kati ya uzao wake,[j] **5** basi
mimi nami nitaukaza uso wa-
ngu juu ya mtu huyo na fa-
milia yake,[k] nami nitamkati-
lia mbali yeye na wote wana-
ofanya uasherati pamoja naye
katika kufanya uasherati[l] na
Moleki watoke katikati ya watu
wao.

SURA 19
a Kut 22:21
b Zek 7:9
c Kum 25:13
Kum 25:15
Met 20:10
d Met 11:1
Met 16:11
e Law 18:5
Kum 4:6

SURA 20
f Law 18:21
Kum 18:10
g 1Pe 3:12
h Kut 15:17
Hes 19:20
Kum 23:14
Eze 5:11
i Law 18:21
j Kum 13:8
k Kut 20:5
1Fa 20:42
l Zb 106:39
Ho 2:13

Safu ya 2
a Law 19:31
Kum 18:11
Ga 5:20
Ufu 21:8
b Law 20:27
Mdo 16:16
c 1Nya 10:13
Eze 6:9
d Law 11:44
Efe 1:4
1Pe 1:16
e Law 18:4
Mhu 12:13
Lu 1:6
f Kut 31:13
Law 21:8
Eze 37:28
1Th 5:23
2Th 2:13
g Kum 27:16
Met 20:20
Mt 15:4
h Kut 21:17
i 2Sa 1:16
1Fa 2:32
j Law 18:20
Kum 5:18
Yer 29:23
Ro 7:3
k Kum 22:22
1Ko 6:9
l Law 18:8
Kum 27:20
m Law 18:15
n Law 18:29
o Mwa 19:5
Law 18:22
Amu 19:22
Ro 1:27
1Ko 6:9
Yud 7
p Law 18:17
Kum 27:23
q Law 21:9

6 "'Nayo nafsi inayowaendea
wenye kuwasiliana na pepo[a] na
wajuzi wa kubashiri[b] matukio
ili kufanya uasherati nao, nita-
uweka uso wangu juu ya nafsi
hiyo na kumkatilia mbali kuto-
ka katikati ya watu wake.[c]
7 "'Nanyi mtajitakasa na
kuwa watakatifu,[d] kwa sababu
mimi ni Yehova Mungu wenu.
8 Nanyi mtazishika sheria za-
ngu na kuzitenda.[e] Mimi ni Ye-
hova, ninayewatakasa ninyi.[f]
9 "'Ikiwa kutakuwa na mtu
yeyote anayemlaani baba yake
na mama yake,[g] lazima auawe.[h]
Ni baba yake na mama
yake ambao amewalaani. Damu
yake mwenyewe iko juu yake.[i]
10 "'Sasa mwanamume ana-
yefanya uzinzi na mke wa
mwanamume mwingine ni
mwanamume anayefanya uzi-
nzi na mke wa mwenzake.[j] La-
zima auawe, mwanamume huyo
mzinzi na vilevile mwanamke
huyo mzinzi.[k] **11** Na mwana-
mume anayelala na mke wa
baba yake ameufunua uchi wa
baba yake.[l] Lazima wote wawi-
li wauawe. Damu yao wenye-
we iko juu yao. **12** Na mwa-
namume akilala na binti-mkwe
wake, lazima wote wawili wau-
awe.[m] Wamevunja jambo la asi-
li. Damu yao wenyewe iko juu
yao.[n]
13 "'Na mwanamume akila-
la na mwanamume sawa na vile
mtu anavyolala na mwanamke,
wote wawili wamefanya jambo
lenye kuchukiza.[o] Lazima wa-
uawe. Damu yao wenyewe iko
juu yao.
14 "'Na mwanamume aki-
mchukua mwanamke pamo-
ja na mama yake, ni mwene-
ndo mpotovu.[p] Watamteketeza
yeye na wao katika moto,[q] ili

mwenendo mpotovu[a] usiendelee katikati yenu.

15 "'Na mwanamume akimpa mnyama shahawa yake imtokayo,[b] lazima auawe, nanyi mtamuua mnyama huyo. **16** Na mwanamke akimkaribia mnyama yeyote ili kuungana[c] naye, mtamuua mwanamke huyo na mnyama huyo. Lazima wauawe. Damu yao wenyewe iko juu yao.

17 "'Na mwanamume akimchukua dada yake, binti ya baba yake au binti ya mama yake, naye auone uchi wake, naye dada yake auone uchi wake, ni aibu.[d] Kwa hiyo watakatiliwa mbali kutoka machoni pa wana wa watu wao. Ni uchi wa dada yake ambao ameufunua. Atajibu kwa kosa lake.

18 "'Na mwanamume akilala na mwanamke mwenye hedhi na kuufunua uchi wake, ameifunua chemchemi yake, naye mwanamke huyo ameifichua chemchemi ya damu yake.[e] Kwa hiyo wote wawili watakatiliwa mbali kutoka katikati ya watu wao.

19 "'Nao uchi wa dada ya mama yako[f] na dada ya baba yako[g] usiufunue, kwa sababu mtu atakuwa ameufunua uhusiano wake wa damu.[h] Watajibu kwa kosa lao. **20** Na mwanamume anayelala na mke wa ndugu ya baba yake ameufunua uchi wa ndugu ya baba yake.[i] Watajibu kwa dhambi yao. Watakufa bila kupata mtoto.[j] **21** Na mtu akimchukua mke wa ndugu yake, ni chukizo.[k] Ni uchi wa ndugu yake ambao ameufunua. Watakuwa bila mtoto.

22 "'Nanyi mtazishika sheria[l] zangu zote na maamuzi yangu yote ya hukumu[a] na kuzifanya, ili nchi nitakayowaingiza mkae ndani yake isije ikawatapika ninyi.[b] **23** Nanyi msitembee katika sheria za mataifa ambayo nitayafukuza kutoka mbele yenu,[c] kwa sababu wamefanya mambo hayo yote nami nayachukia.[d] **24** Ndipo nikawaambia ninyi:[e] "Ninyi mtaimiliki nchi yao, nami nitawapa ninyi ili mwimiliki, nchi inayotiririka maziwa na asali.[f] Mimi ni Yehova Mungu wenu, ambaye nimewatenga kutoka kwa vikundi vya watu."[g] **25** Nanyi mtatofautisha mnyama aliye safi na asiye safi na kutofautisha ndege aliye safi na asiye safi;[h] nanyi msizifanye nafsi zenu kuwa zenye kuchukiza[i] kupitia mnyama na ndege na kitu chochote ambacho hutembea juu ya nchi ambacho nimekitenga kwa ajili yenu kwa kuvitangaza kuwa si safi. **26** Nanyi mtakuwa watakatifu kwangu,[j] kwa sababu mimi Yehova ni mtakatifu;[k] nami ninawatenga kutoka kwa vikundi vya watu ili muwe wangu.[l]

27 "'Naye mwanamume au mwanamke atakayekuwa na roho ya kuwasiliana na pepo au roho ya kubashiri,[m] lazima wauawe.[n] Watawapiga hao kwa mawe na kuwaua. Damu yao wenyewe iko juu yao.'"[o]

21 Na Yehova akaendelea kumwambia Musa: "Ongea na makuhani, wana wa Haruni, nawe uwaambie, 'Kwa ajili ya nafsi iliyokufa, mtu yeyote asijitie unajisi katikati ya watu wake.[p] **2** Lakini kwa ajili ya mtu mwenye uhusiano wa damu aliye karibu naye, kwa ajili ya mama yake na kwa ajili ya baba yake na kwa ajili

SURA 20

a Ga 5:19
b Kut 22:19
Kum 27:21
c Law 18:23
d Law 18:9
Kum 27:22
2Sa 13:12
Eze 22:11
e Law 15:24
Law 18:19
Eze 22:10
f Law 18:13
g Law 18:12
h Law 18:6
i Law 18:14
j Zb 109:13
k Law 18:16
Kum 25:5
Mk 6:18
Mk 12:19
l Law 18:26
Zb 105:45
Zb 119:80
Mhu 12:13

Safu ya 2

a Kut 21:1
Kum 5:1
Zb 119:20
Isa 26:9
b Law 18:28
c Law 18:3
Law 18:24
Kum 12:30
Yer 10:2
d Law 18:27
Kum 9:5
e Kut 3:17
Kut 6:8
f Kum 8:8
Eze 20:6
g Kut 19:5
Kut 33:16
1Fa 8:53
2Ko 6:16
1Pe 2:9
h Law 11:47
Kum 14:4
Mdo 10:14
i Law 11:43
j Law 19:2
k Zb 99:5
1Pe 1:16
Ufu 4:8
l Kum 7:6
Kum 14:2
Tit 2:14
m Kut 22:18
Law 19:31
Kum 18:10
1Sa 28:7
Ufu 21:8
n Kut 22:18
Law 20:6
Mik 5:12
o 2Sa 1:16

SURA 21

p Hes 19:14

ya mwana wake na kwa ajili
ya binti yake na kwa ajili ya
ndugu yake **3** na kwa ajili ya
dada yake, bikira aliye karibu
naye, ambaye hajawa wa mwa-
namume, kwa ajili yake ana-
weza kujitia unajisi. **4** Hataji-
tia unajisi kwa ajili ya mwa-
namke mwenye mume katikati
ya watu wake ili kujitia unajisi.
5 Hawataweka upara juu ya vi-
chwa[a] vyao, na ncha ya nde-
vu zao hawatanyoa,[b] na katika
mwili wao hawatafanya mka-
to.[c] **6** Watakuwa watakatifu
kwa Mungu wao,[d] nao hawata-
litia unajisi jina la Mungu wao,[e]
kwa sababu wao ndio wanaotoa
matoleo ya Yehova yanayoto-
lewa kwa njia ya moto, mkate
wa Mungu wao;[f] nao watuku-
wa watakatifu.[g] **7** Kahaba[h]
au mwanamke aliyenajisiwa ha-
watamwoa; na mwanamke ali-
yetalikiwa[i] kutoka kwa mume
wake hawatamwoa,[j] kwa saba-
bu yeye ni mtakatifu kwa Mu-
ngu wake. **8** Basi utamtaka-
sa,[k] kwa sababu yeye ni mtu
anayeutoa mkate wa Mungu
wako. Atakuwa mtakatifu kwa-
ko,[l] kwa sababu mimi Yehova,
ninayewatakasa ninyi, mimi ni
mtakatifu.[m]

9 "'Sasa ikiwa binti ya ku-
hani atajitia unajisi kwa kufa-
nya ukahaba, anamtia unajisi
baba yake. Binti huyo atateke-
tezwa katika moto.[n]

10 "'Naye kuhani mkuu wa
ndugu zake ambaye kichwa
chake kimemiminiwa mafuta[o]
na ambaye mkono wake ume-
jazwa nguvu ili kuvaa yale ma-
vazi,[p] hatakiacha kichwa cha-
ke bila kutunzwa,[q] wala hataya-
rarua mavazi yake.[r] **11** Naye
hatakuja mahali penye nafsi
yoyote iliyokufa.[s] Kwa ajili ya

SURA 21
a Kum 14:1
Isa 15:2
Eze 44:20
b Law 19:27
Yer 48:37
c Law 19:28
1Fa 18:28
Yer 16:6
d Kut 29:44
Law 10:3
Ezr 8:28
e Law 18:21
Law 19:12
Law 22:32
f Law 3:11
Mal 1:7
g Isa 52:11
1Pe 1:16
h Law 19:29
i Kum 24:1
Mt 19:8
j Eze 44:22
k Kut 28:41
Law 20:8
1Ko 6:11
Ebr 9:13
l Law 11:44
m Kut 28:36
Law 11:45
Law 20:7
Isa 43:15
n Mwa 38:24
Law 20:14
o Law 8:12
Hes 35:25
Zb 133:2
p Kut 28:2
Kut 29:29
Law 16:32
q Law 10:6
r Mwa 37:34
s Hes 6:7
Hes 19:11
Hes 19:14

Safu ya 2
a Law 10:7
Law 21:23
b Law 8:12
Lu 4:18
Mdo 10:38
c Eze 44:22
2Ko 11:2
Ufu 14:4
d Ezr 9:2
e 1Th 5:23
2Th 2:13
f Law 22:21
Ro 12:1
Efe 5:27
Ebr 7:26
Ufu 14:5
g Law 3:11
Hes 16:5
h Law 22:23
i Law 22:24
Kum 23:1
j Law 2:2
k Law 22:25
l Law 2:10
Law 6:16
Law 24:9
Hes 18:9

baba yake na mama yake ha-
tajitia unajisi. **12** Pia hatato-
ka nje ya patakatifu wala ku-
patia unajisi patakatifu pa Mu-
ngu wake,[a] kwa sababu ishara
ya wakfu, yale mafuta ya Mu-
ngu wake yanayotumiwa kutia
mafuta,[b] yako juu yake. Mimi ni
Yehova.

13 "'Naye atamwoa mwana-
mke katika ubikira wake.[c]
14 Na mwanamke mjane au ali-
yetalikiwa na yule aliyenaji-
siwa, kahaba, asimwoe yeyote
kati ya hawa, lakini aoe bikira
kutoka kwa watu wake awe
mke wake. **15** Naye hatautia
unajisi uzao wake kati ya watu
wake,[d] kwa sababu mimi ni Ye-
hova ninayemtakasa.'"[e]

16 Na Yehova akaendelea
kusema na Musa, na kumwa-
mbia: **17** "Sema na Haruni,
na kumwambia, 'Mtu yeyote
wa uzao wako katika vizazi
vyao vyote ambaye ana kaso-
ro[f] asije karibu ili kuutoa mka-
te wa Mungu wake.[g] **18** Ikiwa
kuna mtu yeyote mwenye ka-
soro, asikaribie: mtu aliye ki-
pofu au kilema au mwenye pua
iliyokatika au mwenye kiungo
kimoja kilicho kirefu mno,[h]
19 au mtu aliyevunjika mguu
au aliyevunjika mkono, **20** au
mwenye kijongo au aliyekonda
au mwenye ugonjwa wa macho
au mwenye vigaga au mwenye
mba au aliyevunjwa mapumbu
yake.[i] **21** Mtu yeyote wa uzao
wa Haruni kuhani ambaye ana
kasoro hatakaribia ili kutoa
matoleo ya Yehova kwa njia ya
moto.[j] Kuna kasoro ndani yake.
Hatakaribia ili kuutoa mkate
wa Mungu wake.[k] **22** Anawe-
za kula mkate wa Mungu wake
kutoka kati ya vitu vitakatifu
zaidi[l] na kutoka kati ya vitu vi-

takatifu.[a] **23** Hata hivyo, hatakaribia pazia,[b] wala hatakaribia madhabahu,[c] kwa sababu kuna kasoro ndani yake;[d] naye hatapatia unajisi patakatifu pangu,[e] kwa kuwa mimi ni Yehova ninayewatakasa wao.'"[f]

24 Basi Musa akasema na Haruni na wanawe na wana wote wa Israeli.

22 Na Yehova akazidi kusema na Musa, na kumwambia: **2** "Sema na Haruni na wanawe, kwamba wajitenge na vitu vitakatifu vya wana wa Israeli nao wasilitie unajisi jina langu takatifu[g] katika vitu ambavyo wananitakasia.[h] Mimi ni Yehova. **3** Waambie, 'Katika vizazi vyenu vyote mtu yeyote wa uzao wenu wote atakayekaribia vitu vitakatifu, ambavyo wana wa Israeli watamtakasia Yehova, wakati ambapo uchafu wake ungali juu yake,[i] nafsi hiyo itakatiliwa mbali kutoka mbele zangu. Mimi ni Yehova. **4** Hakuna mtu yeyote wa uzao wa Haruni wakati ambapo ana ukoma[j] au mtiririko unaotoka[k] atakayekula vitu vitakatifu mpaka atakapokuwa safi,[l] wala yule atakayegusa mtu yeyote asiye safi kwa nafsi iliyokufa[m] au mtu ambaye shahawa itamtoka,[n] **5** wala mtu atakayegusa kitu chochote kinachozaana kwa wingi ambacho si safi kwake[o] au atakayemgusa mtu asiye safi kwake kuhusiana na uchafu wake wowote.[p] **6** Nafsi itakayogusa kitu chochote cha vitu hivyo itakuwa si safi mpaka jioni naye hatakula kitu chochote katika vitu vitakatifu, lakini ataoga mwili wake katika maji.[q] **7** Jua likiisha kutua, yeye pia atakuwa safi, na baadaye anaweza kula sehemu ya vitu vitakatifu, kwa sababu ni mkate wake.[a] **8** Pia hatakula mwili wowote uliokufa tayari au kitu chochote kilichoraruliwa na wanyama-mwitu na kuwa asiye safi kutokana nacho.[b] Mimi ni Yehova.

9 "'Nao watashika wajibu wao kwangu, wasije wakachukua dhambi kwa sababu yake nao wakafa[c] kwa sababu yake kwa sababu walikuwa wakivitia unajisi. Mimi ni Yehova ninayewatakasa wao.

10 "'Na hakuna mgeni yeyote atakayekula kitu chochote kilicho kitakatifu.[d] Hakuna mkaaji aliye pamoja na kuhani wala mfanyakazi wa kukodiwa atakayekula kitu chochote kilicho kitakatifu. **11** Lakini ikiwa kuhani atanunua nafsi, akifanya ununuzi kwa pesa zake, anaweza kushiriki kukila. Nao watumwa waliozaliwa katika nyumba yake, wanaweza kushiriki kuula mkate wake.[e] **12** Na ikiwa binti ya kuhani atakuwa wa mwanamume aliye mgeni, yeye binti huyo hatakula mchango wa vitu vitakatifu. **13** Lakini ikiwa binti ya kuhani atakuwa mjane au kutalikiwa akiwa hana uzao, naye arudi nyumbani kwa baba yake kama katika ujana wake,[f] anaweza kula sehemu ya mkate wa baba yake;[g] lakini hakuna mgeni yeyote atakayeula.

14 "'Sasa ikiwa mtu atakula kitu kitakatifu bila kukusudia,[h] basi ataongeza sehemu yake ya tano[i] juu yake naye atampa kuhani hicho kitu kitakatifu. **15** Kwa hiyo hawatatia unajisi vitu vitakatifu vya wana wa Israeli, ambavyo huenda wakamchangia Yehova,[j]

SURA 21
a Law 22:10
Hes 18:19
b Kut 30:6
Ebr 10:20
c Kut 38:1
d Law 21:17
e Kut 25:8
Law 21:12
f Kut 28:41

SURA 22
g Law 21:6
Zb 83:18
Zb 135:13
h Kut 28:38
Hes 18:32
Kum 15:19
i Law 7:20
j Law 13:2
k Law 15:2
l Law 14:2
Law 15:13
m Law 21:1
Hes 19:11
Hes 19:22
n Law 15:16
o Law 11:24
Law 11:43
p Law 15:7
Law 15:19
q Hes 19:7
1Ko 6:11
Ebr 10:22

Safu ya 2
a Law 21:22
Hes 18:11
b Kut 22:31
Law 17:15
Kum 14:21
c Kut 28:43
Law 10:2
d Kut 29:33
Mt 12:4
e Hes 18:11
f Mwa 38:11
g Law 10:14
Hes 18:19
h Law 5:15
i Law 5:16
Law 27:13
j Hes 18:32
Eze 22:26

16 na kuwafanya wapate adhabu ya hatia kwa sababu ya kula kwao vitu vyao vitakatifu; kwa maana mimi ni Yehova ninayewatakasa wao.'"

17 Na Yehova akaendelea kusema na Musa, na kumwambia: **18** "Sema na Haruni na wanawe na wana wote wa Israeli, nawe uwaambie, 'Mtu yeyote wa nyumba ya Israeli au mkaaji mgeni katika Israeli anayetoa toleo lake,[a] kwa ajili ya nadhiri[b] yao yoyote au kwa ajili ya matoleo yao ya hiari,[c] ambayo huenda wakamtolea Yehova kwa ajili ya toleo la kuteketezwa, **19** ili kupata kibali[d] kwa ajili yenu, lazima awe hana kasoro,[e] wa kiume kutoka katikati ya mifugo, katikati ya wanakondoo dume au katikati ya mbuzi. **20** Kitu chochote chenye kasoro hamtakitoa,[f] kwa sababu hakitawaletea ninyi kibali.

21 "'Na ikiwa mtu atamtolea Yehova dhabihu ya ushirika[g] ili kulipa nadhiri[h] au kama toleo la hiari, atakuwa asiye na kasoro katikati ya mifugo au kundi, ili kupata kibali. Kasoro yoyote isiwe ndani yake. **22** Hakuna dhabihu yoyote iliyo na upofu au mvunjiko au mkato au chunjua au vigaga au mba,[i] yeyote kati ya hao msimtolee Yehova, wala hakuna toleo lolote linalotolewa kwa njia ya moto[j] kutoka kati ya hao mtakaloweka juu ya madhabahu ya Yehova. **23** Na kuhusu ng'ombe-dume au kondoo mwenye kiungo kirefu mno au kifupi mno,[k] unaweza kumtoa awe toleo la hiari; lakini kwa ajili ya nadhiri hatapokewa kwa kibali. **24** Lakini mwenye mapumbu[l] yaliyominywa au yaliyovunjwa au yaliyong'olewa au yaliyokatwa hamtamtolea Yehova, na katika nchi yenu hamtawatoa. **25** Na yeyote kati ya hao kutoka katika mkono wa mgeni hamtamtoa awe mkate wa Mungu wenu, kwa sababu uharibifu wao umo ndani yao. Kuna kasoro[a] ndani yao. Hawatakubaliwa kwa ajili yenu nanyi mpate kibali.'"[b]

26 Na Yehova akazidi kusema na Musa, na kumwambia: **27** "Ng'ombe-dume au mwanakondoo dume au mbuzi akizaliwa, basi atakaa na mama yake siku saba,[c] lakini kuanzia siku ya nane na kuendelea atapokewa kwa kibali kama toleo, toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto. **28** Naye ng'ombe na kondoo, hamtamchinja yeye pamoja na mtoto wake katika siku moja.[d]

29 "Na ikiwa mtatoa dhabihu ya shukrani kwa Yehova,[e] mtaitoa ili kupata kibali kwa ajili yenu. **30** Katika siku hiyo italiwa.[f] Hamtaacha yoyote mpaka asubuhi.[g] Mimi ni Yehova.

31 "Nanyi mtazishika amri zangu na kuzitenda.[h] Mimi ni Yehova. **32** Nanyi hamtalitia unajisi jina langu takatifu,[i] nami nitatakaswa katikati ya wana wa Israeli.[j] Mimi ni Yehova ninayewatakasa ninyi,[k] **33** Mimi ninayewatoa katika nchi ya Misri ili kujionyesha kuwa Mungu kwenu.[l] Mimi ni Yehova."

23 Na Yehova akaendelea kusema na Musa, na kumwambia: **2** "Sema na wana wa Israeli, nawe uwaambie, 'Sherehe za majira[m] za Yehova ambazo mtatangaza[n] ni miku-

SURA 22
a Hes 15:14
Hes 15:16
b Law 7:16
Law 23:38
Hes 15:3
Zb 22:25
Zb 56:12
c Kum 12:6
d Law 7:18
Law 23:11
e Law 1:3
Law 22:22
f Kum 15:21
Kum 17:1
Mal 1:8
Ebr 9:14
1Pe 1:19
g Law 3:1
h Hes 15:8
Kum 23:21
Zb 50:14
Zb 61:8
Mhu 5:4
i Kum 15:21
Mal 1:8
j Law 3:3
Law 3:14
k Law 21:18
l Law 21:20
Kum 23:1

Safu ya 2
a Law 21:21
b Law 7:18
Law 19:7
c Kut 22:30
d Kut 23:19
Kum 22:6
Met 12:10
e Law 7:12
Zb 107:22
Zb 116:17
Amo 4:5
f Law 7:15
g Kut 12:10
h Law 19:37
Hes 15:40
Kum 4:40
i Law 18:21
Law 19:12
Amo 2:7
j Law 10:3
Isa 29:23
Lu 11:2
k Kut 19:5
Law 20:8
Law 21:8
Yoh 17:17
l Kut 6:7
Law 11:45
Hes 15:41

SURA 23
m Kut 23:14
Law 23:37
n Hes 10:10

sanyiko mitakatifu. Hizi ndizo
sherehe zangu za majira:
3 "'Siku sita kazi inaweza
kufanywa, lakini katika siku ya
saba ni sabato ya pumziko ka-
mili,[a] mkusanyiko mtakatifu.
Hamtafanya kazi ya aina yoyo-
te. Ni sabato kwa Yehova kati-
ka makao yenu yote.[b]
4 "'Hizi ndizo sherehe za ma-
jira[c] za Yehova, mikusanyiko
mitakatifu,[d] ambazo mtatanga-
za katika wakati wake ulio-
wekwa:[e] **5** Katika mwezi wa
kwanza, katika siku ya kumi
na nne ya mwezi huo,[f] katika-
ti ya zile jioni mbili ni pasaka[g]
kwa Yehova.
6 "'Na katika siku ya kumi
na tano ya mwezi huu ni she-
rehe kwa Yehova ya keki zisi-
zo na chachu.[h] Kwa siku saba
mtakula keki zisizo na chachu.[i]
7 Katika siku ya kwanza mta-
fanya mkusanyiko mtakatifu.[j]
Hamtafanya kazi ngumu ya
aina yoyote. **8** Lakini mtatoa
toleo linalotolewa kwa Yeho-
va kwa njia ya moto kwa siku
saba. Katika siku ya saba kuta-
kuwa na mkusanyiko mtakati-
fu. Hamtafanya kazi ngumu ya
aina yoyote.'"
9 Na Yehova akaendelea ku-
sema na Musa, na kumwambia:
10 "Sema na wana wa Israe-
li, nawe uwaambie, 'Mwisho-
we mtakapoingia katika nchi
ambayo nitawapa ninyi, nanyi
mtakapokuwa mmevuna ma-
vuno yake, mtaleta pia mga-
nda wa matunda ya kwa-
nza[k] ya mavuno yenu kwa ku-
hani. **11** Naye atautikisa huo
mganda huku na huku,[l] mbe-
le za Yehova ili kupata kiba-
li kwa ajili yenu. Siku itakayo-
fuata sabato kuhani atauti-
kisa huku na huku. **12** Na

SURA 23
a Kut 16:30
Kut 20:10
Law 19:3
Mdo 15:21
b Ne 13:22
Isa 56:2
Isa 58:13
c Kut 23:14
d Kut 12:16
Hes 29:12
e Hes 9:2
f Hes 9:3
Hes 28:16
g Kut 12:6
Kum 16:1
Yos 5:10
1Ko 5:7
h Hes 28:17
Mdo 12:3
1Ko 5:8
i Kut 12:15
Kut 13:6
Kut 34:18
j Kut 12:16
k Hes 18:12
Met 3:9
Eze 44:30
1Ko 15:20
Yak 1:18
l Law 23:15
1Ko 15:20
1Ko 15:23

Safu ya 2
a Yos 5:11
b Kut 34:22
Kum 16:9
c Mdo 2:1
d Hes 28:26
Kum 16:16
e Efe 2:16
Efe 2:18
f Law 7:13
Ro 5:12
g Kut 23:16
Kut 34:22
Yak 1:18
Ufu 14:4
h Hes 28:27

katika siku ambayo mganda
wenu utatikiswa huku na huku
mtamtoa mwana-kondoo dume
ambaye hana kasoro, aliye kati-
ka mwaka wake wa kwanza,
kwa ajili ya toleo la kuketete-
zwa kwa Yehova; **13** na kama
toleo lake la nafaka, sehemu
mbili za kumi za efa ya unga la-
ini uliotiwa mafuta, kama toleo
linalotolewa kwa Yehova kwa
njia ya moto, harufu ya kutuli-
za; na kama toleo lake la ki-
nywaji, sehemu ya nne ya hini
ya divai. **14** Nanyi hamtaku-
la mkate wowote wala nafaka
iliyochomwa wala nafaka mpya
mpaka siku hiyo,[a] mpaka mta-
kapoleta toleo la Mungu wenu.
Ni sheria mpaka wakati usio na
kipimo kwa vizazi vyenu vyote
katika makao yenu yote.
15 "'Nanyi mtajihesabia
toka siku inayofuata sabato,
toka siku ya kuleta kwenu ule
mganda wa toleo la kutikisa,
sabato 7.[b] Zitakuwa kamili.
16 Mpaka siku inayofuata sa-
bato ya 7 mtahesabu, siku 50,[c]
nanyi mtamtolea Yehova to-
leo jipya la nafaka.[d] **17** Ku-
toka katika makao yenu mta-
leta mikate[e] miwili iwe toleo
la kutikisa. Itakuwa ya sehe-
mu mbili za kumi za efa ya
unga laini. Itaokwa ikiwa ime-
tiwa chachu,[f] kama matunda
ya kwanza yaliyoiva kwa Yeho-
va.[g] **18** Nanyi mtatoa pamo-
ja na mikate hiyo wana-kondoo
dume[h] saba ambao hawana ka-
soro, kila mmoja mwenye umri
wa mwaka mmoja, na ng'o-
mbe-dume mmoja mchanga na
kondoo-dume wawili. Wataku-
wa toleo la kuketetezwa kwa
Yehova pamoja na toleo lao
la nafaka na matoleo yao
ya vinywaji yanayotolewa kwa
njia ya moto, yenye harufu ya

kumtuliza Yehova. **19** Nanyi
mtamtoa mwana-mbuzi[a] mmo-
ja awe toleo la dhambi na wana-
kondoo dume wawili, kila mmo-
ja akiwa na umri wa mwaka
mmoja, wawe dhabihu ya ushi-
rika.[b] **20** Naye kuhani atawa-
tikisa huku na huku[c] pamoja na
ile mikate ya matunda ya kwa-
nza yaliyoiva, kama toleo la ku-
tikisa mbele za Yehova, pamo-
ja na wale wana-kondoo dume
wawili. Hivyo vitakuwa vitu
vitakatifu kwa Yehova kwa aji-
li ya kuhani.[d] **21** Nanyi mta-
toa tangazo[e] siku hiyo; kuta-
kuwa na mkusanyiko mtakati-
fu kwa ajili yenu. Hamtafanya
kazi ngumu ya aina yoyote. Ni
sheria mpaka wakati usio na ki-
pimo katika makao yenu yote
kwa vizazi vyenu vyote.

22 "'Na wakati mnapovuna
mavuno ya nchi yenu, hutama-
liza kabisa ukingo wa shamba
lako unapovuna, na masalio
ya mavuno yako hutaokota.[f]
Utayaacha kwa ajili ya watu
wenye kuteseka[g] na mkaaji
mgeni.[h] Mimi ni Yehova Mungu
wenu.'"

23 Na Yehova akaendelea
kusema na Musa, na kumwa-
mbia: **24** "Sema na wana wa
Israeli, na kuwaambia, 'Kati-
ka mwezi wa saba,[i] siku ya kwa-
nza ya mwezi huo, mtakuwa
na pumziko kamili, ukumbusho
kwa kupiga tarumbeta,[j] mku-
sanyiko mtakatifu.[k] **25** Ha-
mtafanya kazi ngumu ya aina
yoyote, nanyi mtamtolea Yeho-
va toleo linalotolewa kwa njia
ya moto.'"

26 Na Yehova akazidi kuse-
ma na Musa, na kumwambia:
27 "Hata hivyo, katika siku ya
kumi ya mwezi huu wa saba
ni siku ya upatanisho.[l] Mtafa-
nya mkusanyiko mtakatifu, na-
nyi mtazitesa nafsi[a] zenu na ku-
mtolea Yehova toleo[b] linalotole-
wa kwa njia ya moto. **28** Na-
nyi hamtafanya kazi ya aina
yoyote siku hiyo, kwa sababu
ni siku ya upatanisho ili kufa-
nya upatanisho[c] kwa ajili yenu
mbele za Yehova Mungu wenu;
29 kwa sababu kila nafsi amba-
yo haitateseka siku hiyo itaka-
tiliwa mbali kutoka kwa watu
wake.[d] **30** Nayo nafsi yoyote
itakayofanya kazi ya aina yo-
yote siku hiyo, mimi nitaihari-
bu nafsi hiyo itoke katikati ya
watu wake.[e] **31** Hamtafanya
kazi ya aina yoyote.[f] Ni sheria
mpaka wakati usio na kipimo
kwa ajili ya vizazi vyenu katika
makao yenu yote. **32** Ni saba-
to ya pumziko kamili kwenu,[g]
nanyi mtazitesa[h] nafsi zenu ka-
tika siku ya tisa ya mwezi huo
wakati wa jioni. Toka jioni mpa-
ka jioni mtaishika sabato."

33 Na Yehova akaendelea
kusema na Musa, na kumwa-
mbia: **34** "Sema na wana wa
Israeli, na kuwaambia, 'Kati-
ka siku ya kumi na tano ya
mwezi huu wa saba ni shere-
he ya vibanda muda wa siku
saba kwa Yehova.[i] **35** Siku ya
kwanza ni mkusanyiko mtaka-
tifu. Hamtafanya kazi ngumu
ya aina yoyote. **36** Siku saba
mtamtolea Yehova toleo linalo-
tolewa kwa njia ya moto. Siku
ya nane mtakuwa na mkusa-
nyiko mtakatifu,[j] nanyi mta-
mtolea Yehova toleo linalotole-
wa kwa njia ya moto. Ni ku-
sanyiko kuu. Hamtafanya kazi
ngumu ya aina yoyote.

37 "'Hizi ndizo sherehe za
majira[k] za Yehova mtakazota-
ngaza kuwa mikusanyiko mi-
takatifu,[l] kwa ajili ya kumtolea

SURA 23

a Law 4:23
Hes 28:30
b Law 3:1
c Law 7:30
d Law 7:34
Law 10:14
Hes 18:9
Kum 18:4
1Ko 9:13
e Hes 10:10
f Law 19:9
Kum 24:19
Ru 2:3
g Isa 58:7
h Law 19:33
Hes 15:15
i 1Fa 8:2
j Hes 10:10
Hes 29:1
k Hes 29:12
l Kut 30:10
Law 16:30
Law 25:9
1Yo 1:7

Safu ya 2

a Law 16:29
Hes 29:7
Zb 35:13
Isa 58:5
b Kum 16:16
Eze 45:17
c Law 16:34
Ebr 9:12
Ebr 9:24
Ebr 9:26
Ebr 10:10
1Yo 2:2
d Hes 9:13
Hes 15:30
e Mdo 3:23
f Law 23:28
Mt 12:12
Mk 3:4
g Law 16:31
h Law 16:29
Law 23:27
Hes 29:7
Zb 35:13
i Kut 23:16
Hes 29:12
Kum 16:13
Ezr 3:4
Ne 8:14
Zek 14:16
Yoh 7:2
j Ne 8:18
Yoh 7:37
k Kut 23:14
Kum 16:16
l Law 23:4
Hes 28:26
Hes 29:7

Yehova toleo linalotolewa kwa
njia ya moto:[a] toleo la kute-
keteza wa[b] na toleo la nafaka[c]
la dhabihu na matoleo ya vi-
nywaji[d] kulingana na ratiba ya
kila siku, **38** mbali na sabato
za Yehova[e] na mbali na zawadi[f]
zenu na mbali na matoleo yenu
ya nadhiri[g] na mbali na mato-
leo yenu ya hiari,[h] ambayo mta-
mtolea Yehova. **39** Hata hi-
vyo, katika siku ya kumi na
tano ya mwezi wa saba, mtaka-
pokuwa mmeyakusanya mazao
ya nchi, mtasherehekea shere-
he[i] ya Yehova siku saba.[j] Kati-
ka siku ya kwanza ni pumziko
kamili na katika siku ya nane
ni pumziko kamili.[k] **40** Na-
nyi mtajichukulia katika siku
ya kwanza tunda la miti ye-
nye fahari, matawi ya mitende[l]
na matawi ya miti yenye maja-
ni mengi na mierebi ya bonde
la mto, nanyi mtashangilia[m]
mbele za Yehova Mungu wenu
siku saba. **41** Nanyi mtaishe-
rehekea kama sherehe kwa Ye-
hova siku saba katika mwa-
ka.[n] Kama sheria mpaka waka-
ti usio na kipimo katika vizazi
vyenu, mtaisherehekea katika
mwezi wa saba. **42** Na kati-
ka vibanda mtakaa siku saba.[o]
Wenyeji wote katika Israe-
li watakaa katika vibanda,[p]
43 ili vizazi vyenu vipate kuju-
a[q] kwamba niliwafanya wana
wa Israeli wakae katika viba-
nda nilipokuwa nikiwatoa kati-
ka nchi ya Misri.[r] Mimi ni Yeho-
va Mungu wenu.'"

44 Basi Musa akawaambia
wana wa Israeli juu ya sherehe[s]
za majira za Yehova.

24 Na Yehova akasema na
Musa, na kumwambia:
2 "Waamuru wana wa Israe-
li wakuletee mafuta safi ya ze-
ituni zilizopondwa kwa ajili ya
mwanga,[a] ili kuiwasha taa da-
ima.[b] **3** Nje ya pazia la Ushu-
huda katika hema la mkuta-
no Haruni ataiweka kwa utara-
tibu toka jioni mpaka asubuhi
mbele za Yehova daima. Ni she-
ria mpaka wakati usio na kipi-
mo katika vizazi vyenu vyote.
4 Juu ya kinara cha taa[c] cha
dhahabu safi ataziweka taa[d]
kwa utaratibu mbele za Yehova
daima.[e]

5 "Nawe utachukua unga la-
ini na kuuoka uwe keki kumi
na mbili za mviringo. Kila keki
itafanyizwa kwa sehemu mbili
za efa. **6** Nawe utaziweka ka-
tika vikundi viwili vya taba-
ka, sita katika kikundi kimo-
ja cha tabaka,[f] juu ya meza ya
dhahabu safi mbele za Yehova.[g]
7 Nawe utaweka ubani safi juu
ya kila kikundi cha tabaka, nao
utakuwa mkate kwa ajili ya ku-
mbukumbu,[h] toleo linalotolewa
kwa Yehova kwa njia ya moto.
8 Katika siku moja ya saba-
to baada ya nyingine atauweka
kwa utaratibu mbele za Yeho-
va daima.[i] Ni agano pamoja na
wana wa Israeli mpaka wakati
usio na kipimo. **9** Nao utaku-
wa wa Haruni na wa wanawe,[j]
nao wataula katika mahali pa-
takatifu,[k] kwa sababu ni kitu
kitakatifu zaidi kwa ajili yake
kutoka kwa matoleo ya Ye-
hova yanayotolewa kwa njia ya
moto, kama sharti mpaka wa-
kati usio na kipimo."

10 Sasa mwana wa mwana-
mke Mwisraeli, ambaye, hata
hivyo, alikuwa mwana wa mwa-
namume Mmisri,[l] akatoka kwe-
nda katikati ya wana wa Israe-
li, naye yule mwana wa mwa-
namke Mwisraeli akaanza ku-
pambana[m] na mwanamume

SURA 23
a Law 1:9; Law 2:2
b Law 1:3
c Law 2:1; Law 2:11
d Kut 29:40; Hes 15:5; Hes 28:7; Flp 2:17
e Kut 16:23; Kut 20:8; Kut 31:13; Isa 56:2
f Kut 28:38; Hes 18:29
g Hes 29:39; Kum 12:11
h Kum 12:6; 1Nya 29:9; 2Nya 35:8; Ezr 2:68
i Zek 14:16; Mt 13:39; Mt 24:31; Mt 25:31
j Kum 16:13
k Law 23:7; Law 23:24; Hes 29:12
l Ne 8:15; Yoh 12:13; Ufu 7:9
m Kum 16:15; Ne 8:10
n Hes 29:12; Ne 8:18
o Kum 31:10
p Ne 8:14; Ne 8:16; Ne 8:17
q Kut 13:14; Kum 31:13; Zb 78:6
r Kut 12:38; Hes 24:5; Zek 14:16
s Law 23:2

Safu ya 2

SURA 24
a Kut 27:20
b Hes 8:2; 2Nya 13:11
c Kut 25:31; Yer 52:19; Ebr 9:2
d Kut 39:37
e Kut 27:20
f Kut 40:23; 1Sa 21:4; Mk 2:26
g Kut 25:24; 1Fa 7:48; Ebr 9:2
h Law 2:2; Law 6:15
i Hes 4:7; 1Nya 9:32; 2Nya 2:4; Ne 10:33
j Law 21:22; Law 22:10; 1Sa 21:6; Mt 12:4; Lu 6:4
k Law 6:16
l Kut 12:38; Hes 11:4
m Kut 2:13

Mwisraeli kambini. **11** Naye
yule mwana wa mwanamke
Mwisraeli akaanza kulitukana
lile Jina[a] na kulilaani.[b] Basi wa-
kamleta kwa Musa.[c] Basi jina
la mama yake lilikuwa Shelomi-
thi, binti ya Dibri wa kabila la
Dani. **12** Ndipo wakamtia ki-
fungoni[d] mpaka kuwe na ta-
ngazo lililo wazi kulingana na
neno la Yehova.[e]

13 Na Yehova akasema
na Musa, na kumwambia:
14 "Mtoe nje ya kambi[f] yule ali-
yelaani; na wale wote waliomsi-
kia wataweka mikono[g] yao juu
ya kichwa chake, nalo kusanyi-
ko lote litampiga kwa mawe.[h]
15 Nawe utasema na wana wa
Israeli, na kuwaambia, 'Ikiwa
mtu yeyote atamlaani Mungu
wake, basi atajibu kwa dha-
mbi yake. **16** Kwa hiyo lazi-
ma yule mtukanaji wa jina la
Yehova auawe.[i] Lazima kusa-
nyiko lote limpige kwa mawe.
Mkaaji mgeni hali kadhalika
mwenyeji atauawa kwa kulitu-
kana lile Jina.[j]

17 "'Na ikiwa mtu ataipiga
nafsi yoyote ya mwanadamu ki-
asi cha kuiua, lazima atauawa.[k]
18 Naye mwenye kuipiga
nafsi ya mnyama wa kufu-
gwa kiasi cha kuiua atalipa,
nafsi kwa nafsi.[l] **19** Na ikiwa
mtu atamtia mwenzake kaso-
ro, basi kama vile tu amba-
vyo yeye amefanya, ndivyo ata-
kavyofanywa.[m] **20** Mfupa uli-
ovunjika kwa mfupa uliovunji-
ka, jicho kwa jicho, jino kwa
jino; aina ileile ya kasoro amba-
yo huenda akamtia mtu, hiyo
ndiyo atakayotiwa.[n] **21** Naye
mwenye kumpiga mnyama kia-
si cha kumuua[o] atalipa,[p] lakini
mwenye kumpiga mwanadamu
kiasi cha kumuua atauawa.[q]

SURA 24
a Zb 8:1
Zb 83:18
Ho 12:5
b Kut 20:7
Kut 21:17
Kut 22:28
Law 19:12
Isa 8:21
Ufu 16:9
c Kut 18:22
d Hes 15:34
e Kut 18:15
f Law 13:46
Hes 5:3
g Kum 13:9
Kum 17:7
h Law 5:1
Hes 15:35
Kum 13:10
i Kum 5:11
j 1Fa 21:10
Zb 74:10
k Mwa 9:6
Kut 21:12
Hes 35:31
Kum 19:13
l Kut 21:35
m Kut 21:23
n Kut 21:24
Kum 19:21
Mt 5:38
o Kut 21:33
p Kut 21:34
Kut 22:1
q Mwa 9:6
Kut 21:12

Safu ya 2
a Kut 12:49
Law 17:10
Law 19:34
Hes 9:14
Hes 15:16
b Ro 3:29
c Hes 15:36
Kum 17:7

SURA 25
d Mwa 15:16
Kum 32:8
Zb 24:1
e Law 26:34
2Nya 36:21
f Kut 23:10
g Kut 23:11
Law 26:34

22 "'Uamuzi mmoja wa hu-
kumu utatumika kwenu. Mkaa-
ji mgeni atakuwa sawa na mwe-
nyeji,[a] kwa sababu mimi ni Ye-
hova Mungu wenu.'"[b]

23 Kisha Musa akasema na
wana wa Israeli, nao waka-
mtoa nje ya kambi yule ali-
yekuwa amelaani, wakampiga
kwa mawe.[c] Basi wana wa Isra-
eli wakafanya kama vile Ye-
hova alivyokuwa amemwamu-
ru Musa.

25 Na Yehova akazidi ku-
sema na Musa kwenye
Mlima Sinai, na kumwambia:
2 "Sema na wana wa Israe-
li, nawe uwaambie, 'Mwishowe
mtakapoingia katika nchi ni-
takayowapa ninyi,[d] ndipo nchi
hiyo itakaposhika sabato kwa
Yehova.[e] **3** Miaka sita utapa-
nda mbegu katika shamba lako,
na miaka sita utakata mata-
wi ya shamba lako la mizabi-
bu, nawe utakusanya mazao ya
nchi.[f] **4** Lakini katika mwaka
wa saba kutakuwa na sabato
ya pumziko kamili kwa ajili ya
nchi hiyo,[g] sabato kwa Yehova.
Shamba lako hutalipanda mbe-
gu, nalo shamba lako la miza-
bibu hutalikata matawi. **5** Mi-
mea inayochipuka kutokana na
mbegu zilizoanguka za mavu-
no yako hutavuna, na zabibu
za mzabibu wako ambao hauja-
katwa matawi usikusanye. Ku-
takuwa na mwaka wa pumzi-
ko kamili kwa ajili ya nchi.
6 Nayo sabato ya nchi itaku-
wa chakula kwa ajili yenu, kwa
ajili yako na mtumwa wako
na kijakazi wako na mfanyaka-
zi wako wa kukodiwa na mkaa-
ji anayekaa pamoja nawe, wale
wanaokaa wakiwa wakaaji wa-
geni pamoja nawe, **7** na kwa
ajili ya mnyama wako wa ku-

fugwa na mnyama-mwitu aliye katika nchi yako. Mazao yake yote yatakuwa ndiyo chakula.

8 "'Nawe utajihesabia sabato 7 za miaka, miaka 7 mara 7, na siku za sabato 7 za miaka zitakuwa miaka 49 kwa ajili yako. **9** Nawe utafanya baragumu ya sauti[a] kubwa ivume katika mwezi wa saba siku ya kumi ya mwezi huo;[b] katika siku ya upatanisho[c] mtaifanya baragumu hiyo ivume katika nchi yenu yote. **10** Nanyi mtautakasa mwaka wa 50 na kutangaza uhuru katika nchi kwa wakaaji wake wote.[d] Itakuwa Yubile[e] kwenu, nanyi mtarudi kila mmoja kwenye miliki yake nanyi mtarudi kila mmoja kwa familia yake.[f] **11** Mwaka wa 50 utakuwa Yubile kwenu.[g] Hamtapanda mbegu wala kuvuna mimea ya nchi inayochipuka kutokana na mbegu zilizoanguka wala kukusanya zabibu kutoka katika mizabibu ambayo haijakatwa matawi.[h] **12** Kwa maana huo ni Yubile. Utakuwa kitu kitakatifu kwenu. Mnaweza kula kutoka shambani kile ambacho nchi inazaa.[i]

13 "'Katika mwaka huu wa Yubile mtarudi kila mmoja kwenye miliki yake.[j] **14** Sasa ikiwa mtamuuzia mwenzenu mali au kununua kutoka katika mkono wa mwenzenu, msikoseane.[k] **15** Kwa hesabu ya miaka iliyo baada ya Yubile utanunua kutoka kwa mwenzako; kwa hesabu ya miaka ya mazao atakuuzia.[l] **16** Kulingana na hesabu kubwa ya miaka ataongeza thamani yake ya ununuzi,[m] na kulingana na uchache wa miaka atapunguza thamani yake ya ununuzi, kwa sababu hesabu ya mazao ndiyo anayokuuzia. **17** Na mtu yeyote kati yenu asimkosee mwenzake,[a] nawe umwogope Mungu wako,[b] kwa sababu mimi ni Yehova Mungu wenu.[c] **18** Kwa hiyo mtazishika sheria zangu na kufuata maamuzi yangu ya hukumu na kuyatenda. Ndipo mtakapokaa katika nchi hiyo kwa usalama.[d] **19** Nayo nchi itatoa mazao yake,[e] nanyi mtakula na kushiba na kukaa kwa usalama juu yake.[f]

20 "'Lakini ikiwa mtasema: "Tutakula nini katika mwaka wa saba kwa kuwa huenda tusipande mbegu wala kukusanya mazao yetu?"[g] **21** ndipo hakika nitaamuru baraka zangu kwa ajili yenu katika mwaka wa sita, nayo itatoa mazao yake kwa ajili ya miaka mitatu.[h] **22** Nanyi mtapanda mbegu mwaka wa nane na mtakula kutokana na mazao ya zamani mpaka mwaka wa tisa. Mtakula yale ya zamani mpaka mazao yake yaingie.

23 "'Kwa hiyo nchi haitauzwa milele,[i] kwa sababu nchi ni yangu.[j] Kwa maana ninyi ni wakaaji wageni na wahamiaji kwa maoni yangu.[k] **24** Na katika nchi yenu yote mnayoimiliki mtaipa nchi haki ya kununuliwa na kurudishwa.[l]

25 "'Ikiwa ndugu yako atakuwa maskini na alazimike kuuza sehemu ya miliki yake, mkombozi wa jamaa yake ya karibu atakuja pia na kununua na kurudisha kile ambacho ndugu yake aliuza.[m] **26** Na ikiwa mtu yeyote hatakuwa na mkombozi nao mkono wake mwenyewe upate faida naye apate kiasi cha kutosha kuikomboa, **27** pia atahesabu miaka tangu alipoiuza naye atarudisha pesa zinazosalia kwa mtu

SURA 25

a Hes 10:2
Hes 10:10
b Law 23:27
c Law 16:30
Law 23:28
d Zb 146:7
Isa 61:1
Isa 63:4
Yer 34:8
Lu 4:18
Ro 8:21
e Law 27:17
Law 27:24
f Law 25:13
Hes 36:4
Kum 15:1
g Mt 12:8
Mt 12:12
Ro 8:21
h Law 25:5
i Kut 23:11
Law 25:6
j Law 25:30
Law 27:24
k 1Sa 12:3
Met 14:31
Amo 5:11
Mik 2:2
1Ko 6:8
l Law 27:18
m Law 27:23

Safu ya 2

a Law 19:13
Met 22:22
Yer 7:6
b Mwa 20:11
Mwa 22:12
Law 25:43
1Sa 12:24
Ne 5:9
Met 1:7
Met 8:13
Mdo 9:31
c Isa 33:22
d Kum 12:10
Zb 4:8
Met 1:33
e Law 26:5
Zb 67:6
Eze 34:27
Yoe 2:24
f Eze 34:25
g Law 25:5
Mt 6:25
h Mwa 26:12
Kum 28:8
Mal 3:10
i 1Fa 21:3
Eze 48:14
j 2Nya 7:20
Zb 24:1
Zb 85:1
Yoe 2:18
k 1Nya 29:15
Zb 39:12
1Pe 2:11
l Law 25:51
m Ru 2:20
Ru 4:4
Ru 4:6
Yer 32:7

aliyemuuzia, naye atarudi kwenye miliki yake.[a]

28 "'Lakini ikiwa mkono wake haupati kiasi cha kutosha kumrudishia, alichokiuza kitaendelea kuwa mkononi mwa mnunuzi wake mpaka mwaka wa Yubile;[b] nacho kitarudishwa katika Yubile, naye atarudi katika miliki yake.[c]

29 "'Sasa ikiwa mtu atauza nyumba ya kukaa katika jiji lenye ukuta, haki yake ya kuikomboa itaendelea pia mpaka mwaka umalizike tangu alipoiuza; haki yake ya kukomboa[d] itaendelea kwa mwaka mzima. **30** Lakini ikiwa haitanunuliwa na kurudishwa kabla ya ule mwaka mzima kutimia kwa ajili yake, nyumba hiyo iliyo katika jiji lenye ukuta itasimama milele ikiwa mali ya mnunuzi katika vizazi vyake. Haitarudishwa katika Yubile. **31** Hata hivyo, nyumba za makao ambayo hayana ukuta kuyazunguka zitahesabiwa kama sehemu ya mashamba ya nchi. Haki ya kukomboa[e] itaendelea kwa ajili yake, na katika Yubile[f] itarudishwa.

32 "'Na kuhusu majiji ya Walawi pamoja na nyumba za majiji ya miliki yao,[g] haki ya kukomboa itaendelea mpaka wakati usio na kipimo kwa ajili ya Walawi.[h] **33** Na mahali ambapo mali ya Walawi hainunuliwi tena, nyumba iliyouzwa katika jiji la miliki yake itatoka pia katika Yubile;[i] kwa sababu nyumba za majiji ya Walawi ni miliki yao katikati ya wana wa Israeli.[j] **34** Tena, kiwanja cha malisho[k] cha majiji yao kisiuzwe, kwa sababu hicho ni miliki mpaka wakati usio na kipimo kwa ajili yao.

SURA 25

a Law 25:50
b Law 25:10
Law 25:13
Law 27:24
c Law 25:10
d Law 25:25
Law 25:51
e Law 25:48
f Law 25:10
g Hes 35:2
Hes 35:8
Yos 21:2
h Yer 32:8
i Law 25:28
j Hes 18:20
Hes 35:4
Kum 18:1
k Hes 35:7
Yos 14:4
Yos 21:2

Safu ya 2

a Law 25:25
Kum 15:7
Zb 41:1
Met 14:20
Met 17:5
Met 19:17
Mk 14:7
b Zb 37:26
Zb 112:5
Met 3:27
Met 14:31
Lu 6:35
Mdo 11:29
1Ti 6:18
1Yo 3:17
c Kut 22:21
Kut 23:9
Law 19:34
Kum 10:18
d Kut 22:25
Kum 23:19
Ne 5:7
Zb 15:5
Met 28:8
Eze 18:13
e Zb 89:7
Met 8:13
Ebr 12:28
f Kum 23:20
Ne 5:10
Lu 6:35
g Kut 20:2
1Fa 8:51
h Kut 6:7
Hes 15:41
i Kut 21:2
Kum 15:12
2Fa 4:1
Ne 5:5
j Kut 1:14
k Law 25:53
1Fa 9:22
l Kut 21:3
Law 25:10
m Kut 19:5
Law 25:55
n Kut 1:13
Kut 3:7
Isa 47:6
Efe 6:9
Kol 4:1
o Kut 1:17
Law 25:17
Mhu 12:13
p Kut 12:38
Yos 9:21

35 "'Na ikiwa ndugu yako atakuwa maskini na kwa hiyo ni dhaifu kifedha karibu nawe,[a] utamtegemeza pia.[b] Kama mkaaji mgeni na kama mhamiaji,[c] ataendelea kukaa akiwa hai pamoja nawe. **36** Usichukue faida na riba kutoka kwake,[d] lakini umwogope Mungu wako;[e] naye ndugu yako ataendelea kukaa akiwa hai pamoja nawe. **37** Hutampa pesa zako kwa faida,[f] wala hutampa chakula chako kwa riba. **38** Mimi ni Yehova Mungu wenu, aliyewatoa ninyi katika nchi ya Misri ili kuwapa nchi ya Kanaani,[g] ili nijionyeshe kuwa Mungu wenu.[h]

39 "'Na ikiwa ndugu yako atakuwa maskini karibu nawe naye alazimike kujiuza kwako,[i] usimtumie kama mfanyakazi katika utumishi wa kitumwa.[j] **40** Atakuwa pamoja nawe kama mfanyakazi wa kukodiwa,[k] kama mhamiaji. Atakutumikia mpaka mwaka wa Yubile. **41** Naye ataondoka kwako, yeye na wanawe pamoja naye, naye atarudi kwa familia yake, naye atarudi kwa miliki ya mababu zake.[l] **42** Kwa maana wao ni watumwa wangu niliowatoa kutoka katika nchi ya Misri.[m] Hawatajiuza kama vile mtumwa anavyouzwa. **43** Hutamkanyagia chini kwa uonevu,[n] nawe utamwogopa Mungu wako.[o] **44** Na kuhusu mtumwa wako na kijakazi wako atakayekuwa wako kutoka katika mataifa yanayowazunguka ninyi, kutoka kwao ninyi mnaweza kununua mtumwa au kijakazi. **45** Na pia kutoka kwa wana wa wahamiaji wanaokaa wakiwa wageni pamoja nanyi,[p] kutoka kwao

mnaweza kuwanunua, na kutoka katika familia zao zilizo pamoja nanyi, waliozaliwa kwao katika nchi yenu; nao watakuwa miliki yenu. **46** Nanyi mtawapitisha wawe urithi kwa wana wenu baada yenu ili wawarithi kama miliki mpaka wakati usio na kipimo.[a] Mnaweza kuwatumia kama wafanyakazi, lakini juu ya ndugu zenu wana wa Israeli, msikanyagane, kwa uonevu.[b]

47 "'Lakini ikiwa mkono wa mkaaji mgeni au mhamiaji aliye pamoja nawe utakuwa na mali, na ndugu yako amekuwa maskini karibu nawe naye alazimike kujiuza kwa mkaaji mgeni au mhamiaji aliye pamoja nawe, au kwa mshiriki wa familia ya huyo mkaaji mgeni, **48** baada ya kujiuza mwenyewe,[c] haki ya kukomboa itaendelea katika kisa chake.[d] Mmoja wa ndugu zake anaweza kumnunua.[e] **49** Au ndugu ya baba yake au mwana wa ndugu ya baba yake anaweza kumnunua, au mtu wa jamaa yake ya kimwili mwenye uhusiano wa damu,[f] mtu wa familia yake, anaweza kumnunua tena.

"'Au ikiwa mkono wake mwenyewe umepata mali, basi mwenyewe atajinunua.[g] **50** Naye atafanya hesabu na mnunuzi wake tangu mwaka aliojiuza mpaka mwaka wa Yubile,[h] na pesa za ununuzi wake zitalingana na hesabu ya miaka.[i] Ataendelea kuwa pamoja naye jinsi ambavyo siku za kazi za mfanyakazi wa kukodiwa huhesabiwa.[j] **51** Ikiwa bado kuna miaka mingi, atalipa bei yake ya ukombozi kulingana nayo kutoka katika pesa zake za ununuzi. **52** Lakini ikiwa ni miaka michache tu inayobaki mpaka mwaka wa Yubile,[a] basi mwenyewe atajipigia hesabu. Kulingana na miaka yake atalipa bei yake ya ukombozi. **53** Ataendelea kuwa pamoja naye kama mfanyakazi wa kukodiwa[b] mwaka baada ya mwaka. Hatamkanyagia chini kwa uonevu[c] mbele ya macho yako. **54** Hata hivyo, ikiwa hawezi kujinunua kwa masharti hayo, atatoka katika mwaka wa Yubile,[d] yeye na wanawe pamoja naye.

55 "'Kwa maana wana wa Israeli ni watumwa wangu.[e] Wao ni watumwa wangu niliowatoa katika nchi ya Misri.[f] Mimi ni Yehova Mungu wenu.[g]

26 "'Msijifanyie miungu isiyo na thamani,[h] wala msijisimamishie sanamu ya kuchongwa[i] au nguzo takatifu, wala msiweke jiwe kuwa sanamu katika[j] nchi yenu ili kuliinamia;[k] kwa maana mimi ni Yehova Mungu wenu. **2** Mtazishika sabato[l] zangu na kupaheshimu patakatifu pangu. Mimi ni Yehova.

3 "'Mkiendelea kutembea katika sheria zangu na kushika amri zangu na kuzifuata,[m] **4** hakika mimi pia nitawapa ninyi manyunyu yenu ya mvua wakati wake unaofaa,[n] nayo nchi itatoa mazao yake,[o] nao mti wa shambani utatoa matunda yake.[p] **5** Na hakika kupura kwenu kutafikia ukusanyaji wenu wa zabibu, nao ukusanyaji wa zabibu utafikia upandaji wa mbegu; na hakika mtakula mkate wenu na kushiba[q] na kukaa kwa usalama katika nchi yenu.[r] **6** Nami nitaweka amani katika nchi,[s] nanyi mtalala, pasipo yeyote wa kuwatemesha;[t] nami nitamkomesha

SURA 25
a Isa 14:2
b Law 25:39
Law 25:43
c Ne 5:5
d Law 25:25
e Ne 5:8
f Ru 2:20
g Law 25:26
1Ko 7:21
h Law 25:10
Law 25:16
i Law 25:27
j Kum 15:18
Isa 16:14
Isa 21:16

Safu ya 2
a Law 25:16
Law 27:18
b Law 25:40
c Law 25:43
Kol 4:1
d Kut 21:3
Law 25:40
e Law 25:42
f Kut 13:3
Kut 20:2
Lu 1:74
g Kum 1:21
Yos 1:9

SURA 26
h Kut 20:4
Law 19:4
Zb 96:5
Mdo 17:29
1Ko 8:4
i Kum 5:8
j Hes 33:52
k Da 3:18
1Ko 10:14
l Law 19:30
m Kum 11:13
Mhu 12:13
Isa 48:18
n Kum 28:12
Isa 30:23
Eze 34:26
Yoe 2:23
Amo 4:7
o Zb 67:6
Zb 85:12
Zek 8:12
p Eze 34:27
Eze 36:30
q Kum 11:15
Yoe 2:19
r Law 25:18
Met 1:33
Yer 23:6
s 1Nya 22:9
Zb 29:11
Hag 2:9
Flp 4:9
t Ayu 11:19
Zb 4:8
Yer 30:10
Mik 4:4

katika nchi[a] mnyama-mwitu
mwenye madhara, nao upanga
hautapita katika nchi yenu.[b]
7 Na hakika ninyi mtawafua-
tilia adui[c] zenu, nao wataa-
nguka kwa upanga mbele yenu.
8 Na hakika watano kati yenu
watawafukuza mia, na mia kati
yenu watawafukuza elfu kumi,
nao adui zenu wataanguka kwa
upanga mbele yenu.[d]
9 "'Nami nitageuka kwenu[e]
na kuwawezesha kuzaana na
kuwazidisha ninyi,[f] nami nita-
timiza agano langu pamoja na-
nyi.[g] **10** Na hakika mtaku-
la vitu vya zamani vya mwaka
uliotangulia,[h] nanyi mtatoa nje
vitu vya zamani kabla ya vitu
vipya. **11** Na hakika mimi ni-
taweka maskani yangu katika-
ti yenu,[i] nayo nafsi yangu hai-
tawachukia ninyi.[j] **12** Na ha-
kika mimi nitatembea katikati
yenu na kujionyesha kuwa Mu-
ngu wenu,[k] nanyi mtajionyesha
kuwa watu wangu.[l] **13** Mimi
ni Yehova Mungu wenu, niliye-
watoa katika nchi ya Misri ili
msiwe watumwa kwao,[m] nami
nikavunja nira zenu na kuwafa-
nya mtembee mkiwa wima.[n]
14 "'Hata hivyo, ikiwa ha-
mtanisikiliza wala kutenda
amri zote hizi,[o] **15** na iki-
wa mtazikataa sheria zangu,[p]
na ikiwa nafsi zenu zitachu-
kia maamuzi yangu ya hukumu
hivi kwamba zisitende amri za-
ngu zote, mfikie hatua ya ku-
livunja agano langu,[q] **16** ndi-
po mimi nitawafanyia yanayo-
fuata, na katika kutoa adha-
bu hakika nitaleta juu yenu
usumbufu kwa kifua kikuu[r] na
homa kali, kufanya macho ya-
fifie[s] na kuifanya nafsi idho-
ofike.[t] Nanyi mtapanda mbe-
gu yenu bure, kwa maana adui
zenu hakika wataila.[a] **17** Na
hakika mimi nitauweka uso
wangu juu yenu, nanyi haki-
ka mtashindwa mbele ya adui
zenu;[b] nao wale wanaowachu-
kia ninyi watawakanyagia chi-
ni,[c] nanyi kwa kweli mtakimbia
wakati ambapo hakuna mtu ye-
yote anayewafuatilia.[d]
18 "'Lakini ikiwa hamtanisi-
kiliza ijapokuwa mambo yote
hayo, ndipo nitawatia adabu
mara saba zaidi kwa sababu ya
dhambi zenu.[e] **19** Nami nita-
kivunja kiburi cha nguvu zenu
na kuzifanya mbingu zenu ziwe
kama chuma[f] na nchi yenu iwe
kama shaba. **20** Nazo nguvu
zenu zitatumika bure, kwa maa-
na nchi yenu haitatoa mazao
yake,[g] nao mti wa dunia hauta-
toa matunda yake.[h]
21 "'Lakini ikiwa mtaende-
lea kutembea kwa kunipi-
nga nanyi msitake kunisiki-
liza mimi, ndipo nitakapoleta
juu yenu mapigo mara saba za-
idi kulingana na dhambi zenu.[i]
22 Nami nitatuma wanyama
wa mwituni katikati yenu,[j] nao
hakika watawaua watoto[k] wenu
na kukatilia mbali wanyama
wenu wa kufugwa na kupu-
nguza hesabu yenu, nazo bara-
bara zenu kwa kweli zitakuwa
ukiwa.[l]
23 "'Hata hivyo, ikiwa kwa
mambo hayo hamtakubali mimi
niwarekebishe[m] na iwe kwamba
ni lazima tu mtembee kwa kuni-
pinga, **24** ndipo mimi, naam,
mimi nitatembea kwa kuwa-
pinga;[n] nami, naam, mimi nita-
wapiga mara saba kwa sababu
ya dhambi zenu.[o] **25** Nami ha-
kika nitaleta juu yenu upanga
unaolipiza kisasi[p] kwa ajili ya
agano;[q] na hakika ninyi mtaji-
kusanya katika majiji yenu,

SURA 26

a 2Fa 17:26
b Eze 14:17
c Zb 18:37
d Kum 28:7
Kum 32:30
Yos 23:10
Amu 7:16
Amu 15:15
1Nya 11:20
e Kut 2:25
2Fa 13:23
f Kum 28:4
Ne 9:23
Zb 107:38
g Kut 6:4
h Law 25:22
i Kut 25:8
Yos 22:19
Eze 37:26
Ufu 21:3
j Law 20:23
Yer 14:21
k Kut 6:7
Kum 23:14
2Ko 6:16
l Yer 7:23
Eze 11:20
m Kut 20:2
Law 25:38
Yer 11:4
n Yer 2:20
o Kum 28:15
Mal 2:2
p 2Fa 17:15
Yer 13:10
q Kut 24:7
Kum 31:16
Yer 11:10
Ebr 8:9
r Kum 28:22
s 1Sa 2:33
t Eze 33:10

Safu ya 2

a Kum 28:33
Amu 6:3
b Kum 28:25
Amu 2:14
1Sa 4:10
Omb 2:17
c Zb 106:41
Omb 1:5
d Law 26:36
Met 28:1
e Law 26:21
Zb 76:7
Zb 79:12
f Kum 11:17
1Fa 17:1
g Yer 12:13
Hag 1:6
h Kum 11:17
Kum 28:18
Hag 1:10
i Law 26:18
j Kum 32:24
2Fa 17:25
Yer 15:3
k 2Fa 2:24
Eze 5:17
l Amu 5:6
Isa 33:8
Eze 14:15
Zek 7:14
m Isa 1:16
Yer 2:30
Yer 5:3
Ebr 12:6
n Ayu 9:4
Zb 18:26
o Law 26:18
p Eze 6:9
Ebr 10:30
q Kut 24:7

nami hakika nitaleta tauni katikati yenu,[a] nanyi mtatiwa mkononi mwa adui.[b] **26** Nitakapokuwa nimevunja fimbo zenu ambazo huning'inizwa mikate ya mviringo,[c] kwa kweli wanawake kumi watataoka mkate wenu katika jiko moja na kuwarudishia mkate wenu kulingana na uzito;[d] nanyi mtakula bali hamtashiba.[e]

27 "'Hata hivyo, ikiwa pamoja na hayo hamtanisikiliza na iwe kwamba ni lazima tu mtembee kwa kunipinga,[f] **28** ndipo nitakapotembea kwa kuwapinga vikali,[g] na mimi, naam, mimi nitawatia adabu mara saba kwa sababu ya dhambi zenu.[h] **29** Kwa hiyo mtakula nyama ya wana wenu, nanyi mtakula nyama ya binti zenu.[i] **30** Na hakika mimi nitaangamiza mahali penu patakatifu pa juu[j] na kuvikatilia mbali vinara vyenu vya uvumba na kuilaza mizoga yenu wenyewe juu ya mizoga ya sanamu zenu za mavi;[k] nayo nafsi yangu itawachukia ninyi.[l] **31** Nami nitayatia majiji yenu kwenye upanga[m] na kufanya ukiwa patakatifu penu,[n] wala sitanusa harufu zenu za kutuliza.[o] **32** Nami nitaifanya nchi iwe ukiwa,[p] nao adui zenu wanaokaa ndani yake wataitazama kwa mshangao.[q] **33** Nami nitawatawanya ninyi katikati ya mataifa,[r] nami nitauchomoa upanga nyuma yenu;[s] nayo nchi yenu itakuwa ukiwa,[t] na majiji yenu yatakuwa bomoko lenye ukiwa.

34 "'Na wakati huo nchi italipa sabato zake siku zote za kukaa kwake ukiwa, huku ninyi mkiwa katika nchi ya adui zenu. Wakati huo nchi itashika sabato, kwa maana lazima ilipe sabato zake.[a] **35** Siku zote za kukaa kwake ukiwa itashika sabato, kwa sababu haikushika sabato wakati wa sabato zenu mlipokuwa mkikaa juu yake.

36 "'Nao wale wanaobaki katikati yenu,[b] hakika nitatia woga mioyoni mwao katika nchi za adui zao; na sauti ya jani linalopeperushwa itawafukuza, nao kwa kweli watakimbia kama wanavyoukimbia upanga na kuanguka pasipo mtu yeyote kufuatilia.[c] **37** Na hakika wao watajikwaa juu ya mmoja na mwenzake kana kwamba ni kutokana na upanga pasipo mtu yeyote kufuatilia, nanyi hamtakuwa na uwezo wowote wa kusimama na kuwapinga adui zenu.[d] **38** Nanyi mtaangamia katikati ya mataifa,[e] nayo nchi ya adui zenu itawala ninyi. **39** Na wale watakaobaki kati yenu, wataoza[f] kabisa kwa sababu ya kosa lao katika nchi za adui zenu. Naam, kwa sababu ya makosa ya baba zao,[g] pamoja nao wataoza kabisa. **40** Na hakika wao wataungama kosa lao wenyewe[h] na kosa la baba zao katika ukosefu wao wa uaminifu walipojiendesha kwa njia isiyo ya uaminifu kunielekea mimi, naam, wakati ambapo walitembea kwa kunipinga.[i] **41** Hata hivyo, mimi nilitembea kwa kuwapinga,[j] na nikalazimika kuwaleta katika nchi ya adui zao.[k]

"'Labda wakati huo moyo wao ambao haujatahiriwa[l] utanyenyekezwa,[m] na wakati huo watalipia kosa lao. **42** Nami nitalikumbuka agano langu

SURA 26

a Kum 28:21
2Sa 24:15
Yer 24:10
Amo 4:10
b Amu 2:14
1Sa 4:10
c Zb 105:16
Eze 5:16
d Eze 4:16
e Isa 9:20
Mik 6:14
Hag 1:6
f Law 26:21
g Isa 59:18
Yer 21:5
h Law 26:18
Law 26:21
i Kum 28:53
2Fa 6:29
Yer 19:9
Omb 2:20
Omb 4:10
Eze 5:10
j 1Fa 13:2
2Fa 23:8
2Nya 34:3
Isa 27:9
k 2Fa 23:20
Yer 16:18
Eze 6:5
l Zb 78:59
m 2Fa 25:9
2Nya 36:17
Ne 2:3
Isa 1:7
Yer 4:7
n Zb 74:7
Yer 52:13
Omb 1:10
Mk 13:2
o Mwa 8:21
p Kum 29:23
Yer 9:11
Lu 21:20
q Kum 28:37
Yer 18:16
Omb 2:15
Eze 5:15
r Zb 44:11
Yer 9:16
s Eze 12:14
t Yer 9:11
Zek 7:14

Safu ya 2

a 2Nya 36:21
b Isa 24:6
c Law 26:17
Met 28:1
Isa 30:17
Eze 21:7
d Yos 7:12
Amu 2:14
Isa 10:4
Yer 37:10
e Kum 4:27
Kum 28:48
Yer 42:17
f Kum 4:27
Kum 28:65
Eze 6:9
g Kut 20:5
Hes 14:18
Kum 5:9
h 1Fa 8:33
Ne 9:2
Da 9:5
i Yer 31:19
Eze 36:31
j Law 26:24
k 1Fa 8:47
2Nya 36:20

l Kum 30:6; Yer 4:4; Yer 9:26; Eze 44:7; Mdo 7:51; Ro 2:29; m 2Nya 12:7.

pamoja na Yakobo;[a] na hata
agano langu pamoja na Isaka[b]
na hata agano langu pamoja
na Abrahamu[c] nitalikumbuka,
nayo nchi nitaikumbuka.
43 Wakati wote huo walipoia-
cha nchi na ilipokuwa ikilipa
sabato zake[d] huku ikikaa ukiwa
bila wao, nao wenyewe wali-
kuwa wakilipia kosa lao,[e] kwa
sababu, naam kwa sababu, wa-
likuwa wameyakataa maamuzi
yangu ya hukumu,[f] nazo nafsi
zao zilikuwa zimechukia sheria
zangu.[g] **44** Na hata hivyo pa-
moja na yote hayo, huku wa-
kiendelea kukaa katika nchi
ya adui zao, hakika sitawakata-
taa[h] wala kuwachukia[i] ili ku-
waangamiza, na kulivunja aga-
no[j] langu pamoja nao; kwa maa-
na mimi ni Yehova Mungu wao.
45 Nami nitakumbuka kwa aji-
li yao lile agano la mababu[k] zao
ambao niliwatoa katika nchi ya
Misri machoni pa mataifa,[l] ili
nijionyeshe kuwa Mungu wao.
Mimi ni Yehova.'"

46 Hayo ndiyo masharti na
maamuzi ya hukumu[m] na she-
ria ambazo Yehova aliweka kati
yake na wana wa Israeli katika
Mlima Sinai kupitia Musa.[n]

27 Na Yehova akaendelea
kusema na Musa, na ku-
mwambia: **2** "Sema na wana
wa Israeli, nawe uwaambie, 'Iki-
wa mtu atamwekea Yehova na-
dhiri ya pekee[o] kwa kumto-
lea Yehova nafsi kulingana na
thamani iliyokadiriwa, **3** nayo
thamani iliyokadiriwa iwe ya
mwanamume mwenye umri wa
kuanzia miaka 20 mpaka mia-
ka 60, basi thamani iliyokadiri-
wa itakuwa shekeli 50 za fedha
kulingana na shekeli ya maha-
li patakatifu. **4** Lakini ikiwa
ni mwanamke, basi thamani ili-
yokadiriwa itakuwa shekeli 30.
5 Na ikiwa umri ni kuanzia mi-
aka 5 mpaka miaka 20, basi
thamani iliyokadiriwa ya mwa-
namume itakuwa shekeli 20 na
kwa ajili ya mwanamke itakuwa
shekeli 10. **6** Na ikiwa umri ni
kuanzia mwezi mmoja mpaka
miaka mitano, basi thamani ili-
yokadiriwa ya mwanamume ita-
kuwa shekeli tano[a] za fedha na
kwa ajili ya mwanamke thama-
ni iliyokadiriwa itakuwa shake-
li tatu za fedha.

7 "'Sasa ikiwa umri ni kuan-
zia miaka 60 na zaidi, ikiwa ni
mwanamume, basi thamani ili-
yokadiriwa itakuwa shekeli 15
na kwa ajili ya mwanamke ita-
kuwa shekeli 10. **8** Lakini iki-
wa amekuwa maskini mno kwa
ajili ya ile thamani iliyokadi-
riwa,[b] ndipo atakapomsimami-
sha mtu huyo mbele ya kuhani,
naye kuhani atakadiria thama-
ni yake.[c] Kulingana na anacho-
weza[d] yule mwenye kuweka na-
dhiri, kuhani atakadiria thama-
ni yake.

9 "'Na ikiwa ni mnyama
kama yule ambaye mtu humto-
lea Yehova, kila kitu ambacho
atampa Yehova kitakuwa kitu
kitakatifu.[e] **10** Hataweka ki-
ngine mahali pake, wala ku-
kibadili chema kwa kibaya au
kibaya kwa chema. Lakini iki-
wa ni lazima akibadili, mnya-
ma kwa mnyama, basi lazima
hicho chenyewe na kile kita-
kachobadilishwa nacho vitaku-
wa kitu kitakatifu. **11** Na iki-
wa ni mnyama yeyote asiye safi[f]
kama yule ambaye mtu hawe-
zi kumtoa katika toleo kwa Ye-
hova,[g] basi lazima amsimami-
she mnyama huyo mbele ya ku-
hani.[h] **12** Naye kuhani ata-
mkadiria thamani yake iwapo

SURA 26
a Mwa 28:13
Hes 32:11
b Mwa 26:3
c Mwa 12:7
Kut 2:24
Kum 4:31
Zb 106:45
Lu 1:72
d Law 26:34
2Nya 36:21
e Law 26:41
Hes 14:34
f 2Fa 17:15
g Law 26:15
h Kum 4:31
2Fa 13:23
Ne 9:31
Ro 11:2
i Law 26:11
j Kum 4:13
Yer 14:21
k Kut 24:3
Kut 24:8
Kum 9:9
l Zb 98:2
Eze 20:9
m Kum 6:1
n Law 27:34
Yoh 1:17

SURA 27
o Hes 6:2
Kum 23:21
Amu 11:30
1Sa 1:11
Mhu 5:4

Safu ya 2
a Hes 18:16
b Law 5:7
Law 5:11
Law 12:8
Law 14:21
c Hes 3:6
2Fa 12:4
d Lu 21:2
2Ko 8:12
e Law 2:3
Hes 18:9
f Law 20:25
Kum 14:7
g Mal 1:11
h Law 10:10
Hes 3:6
Eze 44:23

ni mzuri au mbaya. Kulingana na thamani iliyokadiriwa na kuhani,[a] ndivyo atakavyokuwa. **13** Lakini ikiwa anataka kumnunua, basi atatoa sehemu yake ya tano[b] kwa kuongezea ile thamani iliyokadiriwa.

14 "'Sasa ikiwa mtu ataitakasa nyumba yake iwe kitu kitakatifu kwa Yehova, basi kuhani atakadiria thamani yake iwapo ni nzuri au mbaya.[c] Kulingana na kadirio la kuhani ambalo ataikadiria, ndivyo itakavyogharimu. **15** Lakini ikiwa mtakasaji anataka kuinunua nyumba yake, basi atatoa sehemu ya tano ya thamani iliyokadiriwa kwa kuongezea thamani hiyo;[d] nayo itakuwa yake.

16 "'Na ikiwa ni sehemu ya shamba lililo mali yake[e] ambalo mtu anataka kulitakasa kwa Yehova, basi thamani itakadiriwa kulingana na mbegu yake: ikiwa ni homeri[f] moja ya mbegu ya shayiri, basi kwa shekeli 50 za fedha. **17** Ikiwa atalitakasa shamba lake kuanzia mwaka wa Yubile[g] na kuendelea, litagharimu kulingana na thamani iliyokadiriwa. **18** Na ikiwa atalitakasa shamba lake baada ya Yubile, basi kuhani atafanya hesabu ya bei kulingana na miaka inayobaki mpaka mwaka wa Yubile inayofuata, na kiasi fulani kitapunguzwa kutoka katika thamani iliyokadiriwa.[h] **19** Lakini ikiwa mtakasaji wake atalinunua shamba hilo, basi atatoa sehemu ya tano ya pesa ya thamani iliyokadiriwa kwa kuongezea thamani hiyo, nalo litaendelea kuwa lake.[i] **20** Sasa ikiwa hatalinunua shamba hilo lakini shamba hilo liuziwe mtu mwingine, halitanunuliwa na kurudishwa tena. **21** Na wakati shamba hilo litakapotoka katika Yubile litakuwa kitu kitakatifu kwa Yehova, kama shamba lililotolewa wakfu.[a] Kuhani atalimiliki.[b]

22 "'Na ikiwa atamtakasia Yehova shamba alilolinunua ambalo si sehemu ya shamba lililo mali yake,[c] **23** basi kuhani atamfanyia hesabu ya kadirio la thamani mpaka mwaka wa Yubile, naye atatoa thamani iliyokadiriwa katika siku hiyo.[d] Ni kitu kitakatifu kwa Yehova.[e] **24** Katika mwaka wa Yubile shamba hilo litarudi kwa mtu aliyelinunua kutoka kwake, kwa mtu ambaye shamba hilo ni mali yake.[f]

25 "'Sasa kila thamani itakadiriwa kwa shekeli ya mahali patakatifu. Shekeli itakuwa gera 20.[g]

26 "'Ila mzaliwa wa kwanza kati ya wanyama, anayezaliwa akiwa mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya Yehova,[h] mtu yeyote asimtakase. Awe ni ng'ombe au kondoo, ni wa Yehova.[i] **27** Na ikiwa ni mmoja wa wanyama wasio safi[j] naye ni lazima amkomboe kulingana na thamani iliyokadiriwa, basi atatoa sehemu yake ya tano kwa kuongezea juu yake.[k] Lakini ikiwa hatanunuliwa, basi atauzwa kulingana na thamani iliyokadiriwa.

28 "'Ila tu hakuna kitu chochote kilichotolewa wakfu ambacho huenda mtu akamtolea Yehova kwa ajili ya uharibifu[l] kutoka katikati ya vyote vilivyo vyake, iwe ni kutoka kwa wanadamu au wanyama au kutoka katika shamba lililo mali yake, kitakachouzwa, wala hakuna aina yoyote ya kitu

SURA 27

a Law 5:15
Law 6:6

b Law 5:16
Law 6:5
Law 22:14
Law 27:19

c Law 27:12

d Law 27:13

e Mdo 4:34

f Eze 45:11
Ho 3:2

g Law 25:10
Law 25:50

h Law 25:15
Law 25:16
Law 25:27

i Law 27:13

Safu ya 2

a Kum 22:9
Eze 44:29

b Hes 18:14

c Law 25:10
Law 25:25

d Law 27:12
Law 27:18

e Law 27:9

f Law 25:28

g Kut 30:13
Hes 3:47
Hes 18:16
Eze 45:12

h Kut 13:2
Hes 18:17

i Kut 22:30
Kum 15:19

j Kum 15:21

k Law 27:13

l Kut 22:20
Kum 7:25
Kum 7:26
Yos 6:17
Yos 7:1
1Sa 15:3

kilichotolewa ambacho kitanunuliwa.[a] Hicho ni kitu kitakatifu zaidi kwa Yehova. **29** Hakuna mtu yeyote ambaye huenda akawa ametengwa kwa ajili ya kuharibiwa kutoka kati ya wanadamu atakayekombolewa.[b] Lazima auawe.[c]

30 "'Na kila sehemu ya kumi[d] ya nchi, kutoka katika mbegu ya nchi na tunda la mti, ni ya Yehova. Ni kitu kitakatifu kwa Yehova. **31** Na ikiwa mtu anataka kununua sehemu yake yoyote ya kumi, atatoa sehemu yake ya tano kwa kuongeza juu ya hiyo.[a] **32** Na kwa kila sehemu ya kumi ya mifugo na ya kundi, kila kitu ambacho hupita chini ya bakora,[b] kichwa cha kumi kitakuwa kitu kitakatifu kwa Yehova. **33** Hatamchunguza iwapo ni mzuri au mbaya, wala hatambadilisha. Lakini akimbadilisha, hicho chenyewe na kile kilichobadilishwa nacho vitakuwa kitu kitakatifu.[c] Hatanunuliwa.'"

34 Hizo ndizo amri[d] ambazo Yehova alimpa Musa kuwa amri kwa wana wa Israeli katika Mlima Sinai.[e]

SURA 27

a Hes 18:14
b Hes 21:2
1Sa 15:18
c 1Sa 15:33
d Mwa 14:20
Mwa 28:22
Hes 18:21
Hes 18:26
Kum 12:6
Kum 14:22
2Nya 31:5
Ne 13:12
Mal 3:10
Lu 11:42
Ebr 7:5

Safu ya 2

a Law 27:13
b Yer 33:13
c Law 27:10
d Law 26:46
Kum 4:45
e Kut 3:1
Hes 1:1
Yoh 1:17

HESABU

1 Naye Yehova akasema na Musa katika nyika ya Sinai,[a] kwenye hema la mkutano,[b] siku ya kwanza ya mwezi wa pili wa mwaka wa pili wa kutoka kwao nchini Misri,[c] naye akamwambia: **2** "Chukueni hesabu[d] ya kusanyiko lote la wana wa Israeli kulingana na familia zao, kulingana na nyumba ya baba zao, kwa hesabu ya majina, wanaume wote, kichwa kwa kichwa kati yao, **3** kuanzia umri wa miaka 20 na zaidi,[e] kila mtu anayeingia jeshini katika Israeli.[f] Mtawaandikisha kulingana na majeshi yao, wewe na Haruni.

4 "Na wanaume fulani watakuwa pamoja nanyi, mwanamume mmoja kwa kabila moja; kila mmoja ni kichwa cha nyumba ya baba zake.[g] **5** Na haya ndiyo majina ya wanaume watakaosimama pamoja nanyi: Wa Rubeni,[h] Elisuri[i] mwana wa Shedeuri; **6** wa Simeoni,[a] Shelumieli[b] mwana wa Zurishadai; **7** wa Yuda,[c] Nashoni[d] mwana wa Aminadabu; **8** wa Isakari,[e] Nethaneli[f] mwana wa Zuari; **9** wa Zabuloni,[g] Eliabu[h] mwana wa Heloni; **10** wa wana wa Yosefu:[i] wa Efraimu,[j] Elishama mwana wa Amihudi; wa Manase,[k] Gamalieli mwana wa Pedazuri; **11** wa Benyamini,[l] Abidani[m] mwana wa Gidioni; **12** wa Dani,[n] Ahiezeri[o] mwana wa Amishadai; **13** wa Asheri,[p] Pagieli[q] mwana wa Okrani; **14** wa Gadi,[r] Eliasafu[s] mwana wa Deueli;[t] **15** wa Naftali,[u] Ahira[v] mwana wa Enani. **16** Hao ndio walioitwa wa kusanyiko, wakuu[w] wa makabila ya baba zao. Hao ndio vichwa vya maelfu ya Israeli."[x]

17 Basi Musa na Haruni wakawachukua wanaume hao waliokuwa wametajwa kwa ma-

SURA 1

a Kut 19:1
Kum 33:2
Mdo 7:38
b Kut 25:22
c Kut 40:17
d Kut 30:12
e Kut 30:14
f Kum 3:18
g Kut 18:25
Hes 1:16
Yos 22:14
Yos 23:2
1Nya 27:1
h Mwa 49:3
i Hes 2:10

Safu ya 2

a Mwa 29:33
Mwa 49:5
b Hes 7:36
c Mwa 29:35
Mwa 49:10
d Ru 4:20
Lu 3:32
e Mwa 30:18
Mwa 49:14
f Hes 10:15
g Mwa 30:20
Mwa 49:13
h Hes 7:24
i Mwa 30:24
Mwa 49:22
1Nya 5:1
j Mwa 41:52
Mwa 48:20
k Mwa 41:51
l Mwa 35:18
Mwa 49:27
m Hes 2:22
n Mwa 30:6
Mwa 49:17
o Hes 7:66
p Mwa 30:13
Mwa 49:20

q Hes 7:72; r Mwa 30:11; Mwa 49:19; s Hes 7:42; Hes 10:20; t Hes 2:14; u Mwa 30:8; Mwa 49:21; v Hes 2:29; Hes 10:27; w Kut 18:21; Hes 7:2; x Kum 1:15.

jina. **18** Nao wakakutanisha
kusanyiko lote katika siku ya
kwanza ya mwezi wa pili, ili
uzao[a] wao utambuliwe kwa ha-
bari ya familia zao katika nyu-
mba ya baba zao, kulingana
na hesabu ya majina, kuanzia
umri wa miaka 20 na zaidi,[b]
kichwa kwa kichwa kati yao,
19 kama vile Yehova alivyoku-
wa amemwamuru Musa; naye
akawaandikisha[c] katika nyika
ya Sinai.

20 Na wana wa Rubeni, mza-
liwa wa kwanza wa Israeli,[d] ku-
zaliwa kwao kulingana na fami-
lia zao katika nyumba ya baba
zao, kukawa kulingana na he-
sabu ya majina, kichwa kwa ki-
chwa kati yao, wanaume wote
wenye umri wa miaka 20 na za-
idi, kila mtu anayeingia jeshini,
21 wale walioandikishwa kati
yao wa kabila la Rubeni waliku-
wa 46,500.[e]

22 Wa wana wa Simeoni,[f] ku-
zaliwa kwao kulingana na fa-
milia zao katika nyumba ya
baba zao, watu wake walioa-
ndikishwa kulingana na hesabu
ya majina, kichwa kwa kichwa
kati yao, wanaume wote wenye
umri wa kuanzia miaka 20 na
zaidi, kila mtu anayeingia jeshi-
ni, **23** wale walioandikishwa
kati yao wa kabila la Simeoni
walikuwa 59,300.[g]

24 Wa wana wa Gadi,[h] kuza-
liwa kwao kulingana na familia
zao katika nyumba ya baba zao
kulingana na hesabu ya majina
kuanzia umri wa miaka 20 na
zaidi, kila mtu anayeingia jeshi-
ni, **25** wale walioandikishwa
kati yao wa kabila la Gadi[i] waliku-
wa 45,650.[j]

26 Wa wana wa Yuda,[k] kuza-
liwa kwao kulingana na familia
zao katika nyumba ya baba zao
kulingana na hesabu ya majina
kuanzia umri wa miaka 20 na
zaidi, kila mtu anayeingia jeshi-
ni, **27** wale walioandikishwa
kati yao wa kabila la Yuda waliku-
wa 74,600.[a]

28 Wa wana wa Isakari,[b] ku-
zaliwa kwao kulingana na fami-
lia zao katika nyumba ya baba
zao kulingana na hesabu ya
majina kuanzia umri wa mia-
ka 20 na zaidi, kila mtu anaye-
ingia jeshini, **29** wale walioa-
ndikishwa kati yao wa kabila la
Isakari walikuwa 54,400.[c]

30 Wa wana wa Zabuloni,[d]
kuzaliwa kwao kulingana na
familia zao katika nyumba ya
baba zao kulingana na hesabu
ya majina kuanzia umri wa mi-
aka 20 na zaidi, kila mtu anaye-
ingia jeshini, **31** wale walioa-
ndikishwa kati yao wa kabila la
Zabuloni walikuwa 57,400.[e]

32 Wa wana wa Yosefu: wa
wana wa Efraimu,[f] kuzaliwa
kwao kulingana na familia zao
katika nyumba ya baba zao ku-
lingana na hesabu ya majina
kuanzia umri wa miaka 20 na
zaidi, kila mtu anayeingia jeshi-
ni, **33** wale walioandikishwa
kati yao wa kabila la Efraimu[g]
walikuwa 40,500.[h]

34 Wa wana wa Manase,[i] ku-
zaliwa kwao kulingana na fami-
lia zao katika nyumba ya baba
zao kulingana na hesabu ya
majina kuanzia umri wa mia-
ka 20 na zaidi, kila mtu anaye-
ingia jeshini, **35** wale walioa-
ndikishwa kati yao wa kabila la
Manase walikuwa 32,200.[j]

36 Wa wana wa Benyami-
ni,[k] kuzaliwa kwao kulinga-
na na familia zao katika nyu-
mba ya baba zao kulingana
na hesabu ya majina kuanzia
umri wa miaka 20 na zaidi,
kila mtu anayeingia jeshini,

SURA 1
a Ezr 2:62
Ne 7:61
b Kut 30:14
Hes 14:29
c Hes 26:2
d Mwa 29:32
Mwa 49:3
Hes 2:10
1Nya 5:1
e Hes 2:11
f Mwa 29:33
Mwa 46:10
Hes 2:12
Hes 26:12
g Hes 2:13
h Mwa 30:11
Mwa 46:16
Hes 26:15
i Hes 26:18
j Hes 2:15
k Mwa 29:35
Mwa 46:12
Mwa 49:10
Hes 2:3
1Nya 5:2
Mt 1:2
Ebr 7:14
Ufu 5:5

Safu ya 2
a Hes 2:4
Hes 26:22
b Mwa 30:18
Mwa 46:13
Hes 2:5
Hes 26:23
c Hes 2:6
d Mwa 30:20
e Hes 2:8
f Mwa 41:52
Mwa 46:20
Mwa 48:19
Hes 2:18
Hes 26:35
Kum 33:17
Amu 12:6
Yer 7:15
g Mwa 48:5
h Hes 2:19
i Hes 2:20
Hes 26:29
j Hes 2:21
k Mwa 43:29
Mwa 46:21
Hes 26:38

37 wale walioandikishwa kati yao wa kabila la Benyamini walikuwa 35,400.[a]

38 Wa wana wa Dani,[b] kuzaliwa kwao kulingana na familia zao katika nyumba ya baba zao kulingana na hesabu ya majina kuanzia umri wa miaka 20 na zaidi, kila mtu anayeingia jeshini, **39** wale walioandikishwa kati yao wa kabila la Dani walikuwa 62,700.[c]

40 Wa wana wa Asheri,[d] kuzaliwa kwao kulingana na familia zao katika nyumba ya baba zao kulingana na hesabu ya majina kuanzia umri wa miaka 20 na zaidi, kila mtu anayeingia jeshini, **41** wale walioandikishwa kati yao wa kabila la Asheri walikuwa 41,500.[e]

42 Wa wana wa Naftali,[f] kuzaliwa kwao kulingana na familia zao katika nyumba ya baba zao kulingana na hesabu ya majina kuanzia umri wa miaka 20 na zaidi, kila mtu anayeingia jeshini, **43** wale walioandikishwa kati yao wa kabila la Naftali walikuwa 53,400.[g]

44 Hao ndio walioandikishwa, ambao Musa aliandikisha, pamoja na Haruni na wakuu wa Israeli, wanaume kumi na wawili. Waliwakilisha kila mmoja nyumba ya baba zake. **45** Na wale wote walioandikishwa wa wana wa Israeli kulingana na nyumba ya baba zao kuanzia umri wa miaka 20 na zaidi, kila mtu anayeingia jeshini katika Israeli, wakawa, **46** naam, wale wote walioandikishwa wakawa 603,550.[h]

47 Hata hivyo, Walawi[i] kulingana na kabila la baba zao hawakuandikishwa kati yao.[j] **48** Kwa hiyo Yehova akasema na Musa, na kumwambia: **49** "Ni kabila la Lawi tu ambalo hutaandikisha, na hesabu yao usiichukue kati ya wana wa Israeli.[a] **50** Na wewe mwenyewe uweke rasmi Walawi juu ya maskani ya Ushuhuda[b] na juu ya vyombo vyake vyote na juu ya kila kitu kilicho chake.[c] Wao wenyewe wataichukua maskani na vyombo vyake vyote,[d] nao wenyewe watahudumu[e] kwenye hiyo maskani; nao watapiga kambi kuizunguka maskani.[f] **51** Na wakati maskani hiyo inapoondoka, Walawi wataishusha; na wakati maskani hiyo inapopiga kambi,[g] Walawi wataisimamisha; na mgeni yeyote anayekaribia anapaswa kuuawa.[h]

52 "Na wana wa Israeli watapiga kambi kila mmoja kulingana na kambi yake, na kila mtu kulingana na mgawanyo[i] wake wa makabila matatu kwa majeshi yao. **53** Nao Walawi watapiga kambi kuizunguka maskani ya Ushuhuda, ili ghadhabu[j] yoyote isizuke juu ya kusanyiko la wana wa Israeli; nao Walawi watashika utumishi wa maskani ya Ushuhuda."[k]

54 Na wana wa Israeli wakafanya kulingana na yote ambayo Yehova alikuwa amemwamuru Musa. Walifanya vivyo hivyo.[l]

2 Sasa Yehova akasema na Musa na Haruni, na kuwaambia: **2** "Wana wa Israeli watapiga kambi, kila mtu kulingana na mgawanyo wake wa makabila matatu,[m] kando ya alama za nyumba ya baba zao. Watapiga kambi kuzunguka pande zote mbele ya hema la mkutano.

3 "Na wale wanaopiga kambi upande wa mashariki kuelekea mapambazuko ya jua watakuwa

SURA 1

a Hes 2:23
b Mwa 30:6
Mwa 46:23
Hes 2:25
Hes 10:25
Hes 26:42
c Hes 2:26
d Mwa 35:26
Hes 2:27
e Hes 2:28
f Mwa 30:8
Mwa 46:24
Hes 26:48
g Hes 2:30
h Mwa 13:16
Mwa 22:17
Mwa 46:3
Kut 12:37
Kut 38:26
Hes 2:32
i Mwa 29:34
Mwa 46:11
Hes 3:12
1Nya 6:1
j Hes 2:33
Hes 26:64

Safu ya 2

a Hes 26:62
b Kut 31:18
c Kut 38:21
Hes 3:8
d Hes 4:15
Hes 4:25
Hes 4:33
e Hes 3:31
Hes 4:12
f Hes 2:17
Hes 3:23
Hes 3:29
Hes 3:35
Hes 3:38
g Hes 10:17
Hes 10:21
h Hes 3:10
Hes 18:22
1Sa 6:19
i Hes 2:2
Hes 2:34
j Law 10:6
Hes 8:19
Hes 16:46
Hes 18:5
k Hes 8:24
Hes 18:3
Hes 31:30
1Nya 23:32
2Nya 13:10
l Kut 39:32

SURA 2

m Hes 1:52
Hes 24:2

l Law 1:3
m Law 2:1
Hes 15:9
n Law 4:3
Ro 8:3
2Ko 5:21
o Law 8:3

wa Israeli wataweka[a] mikono yao juu ya Walawi.[b] **11** Na
Haruni atawasogeza Walawi
huku na huku mbele za Yehova
kama toleo la kutikisa[c] kutoka
kwa wana wa Israeli, nao wata-
endeleza utumishi wa Yehova.[d]
12 "Kisha Walawi wataweka
mikono yao juu ya vichwa vya
wale ng'ombe-dume.[e] Baada ya
jambo hilo, mtoe mmoja awe to-
leo la dhambi na yule mwingine
awe toleo la kuteketezwa kwa
Yehova ili kufanya upatanisho[f]
kwa ajili ya Walawi. **13** Nawe
utawasimamisha Walawi mbele
ya Haruni na wanawe na kuwa-
sogeza huku na huku kama to-
leo la kutikisa kwa Yehova.
14 Nawe utawatenga Walawi
kutoka katikati ya wana wa
Israeli, nao Walawi watakuwa
wangu.[g] **15** Na baadaye Wala-
wi wataingia ndani ili kutumi-
kia katika hema la mkutano.[h]
Kwa hiyo utawatakasa na ku-
wasogeza huku na huku kama
toleo la kutikisa.[i] **16** Kwa
maana wao ni watu waliokabi-
dhiwa, niliokabidhiwa mimi
kati ya wana wa Israeli.[j] Bada-
la ya wale wote wanaofungua
tumbo la uzazi, wazaliwa wote
wa kwanza kati ya wana wa
Israeli,[k] nitawachukua kwa aji-
li yangu mwenyewe. **17** Kwa
maana kila mzaliwa wa kwa-
nza kati ya wana wa Israe-
li ni wangu, kati ya mwanada-
mu na kati ya mnyama.[l] Ka-
tika siku niliyompiga na ku-
muua kila mzaliwa wa kwanza
katika nchi ya Misri[m] niliwa-
takasa hao kwa ajili yangu.[n]
18 Nami nitawachukua Wala-
wi badala ya wazaliwa wote
wa kwanza kati ya wana wa
Israeli.[o] **19** Nami nitamkabi-
dhi Haruni na wanawe hao Wa-
lawi wakiwa watu waliokabi-
dhiwa katikati ya wana wa Isra-
eli,[a] ili kuendeleza utumishi wa
wana wa Israeli katika hema la
mkutano[b] na kufanya upatani-
sho kwa ajili ya wana wa Israe-
li, ili pigo lolote lisitukie katika-
ti ya wana wa Israeli[c] kwa saba-
bu wana wa Israeli wanapakari-
bia mahali patakatifu."
20 Naye Musa na Haruni na
kusanyiko lote la wana wa Isra-
eli wakawafanyia Walawi hi-
yo. Kulingana na yote ambayo
Yehova alikuwa amemwamu-
ru Musa kuhusu Walawi, hivyo
ndivyo wana wa Israeli wali-
vyowafanyia. **21** Basi Walawi
wakajitakasa[d] na kufua mavazi
yao, kisha Haruni akawasogeza
huku na huku kama toleo la ku-
tikisa mbele za Yehova.[e] Hala-
fu Haruni akafanya upatanisho
kwa ajili yao ili kuwatakasa.[f]
22 Mara tu baada ya jambo hilo
Walawi wakaingia ndani ili ku-
endeleza utumishi wao katika
hema la mkutano mbele ya Ha-
runi na wanawe.[g] Kama vile Ye-
hova alivyokuwa amemwamu-
ru Musa kuhusu Walawi, ndi-
yo walivyowafanyia.
23 Sasa Yehova akasema
na Musa, na kumwambia:
24 "Jambo hili linawahusu Wa-
lawi: Kuanzia umri wa miaka 25
na zaidi, ataingia katika ushiri-
ka katika utumishi wa hema la
mkutano. **25** Lakini baada ya
umri wa miaka 50 atatoka ka-
tika ushirika wa utumishi naye
hatatumikia tena. **26** Naye
atawahudumia ndugu zake ka-
tika hema la mkutano kwa ku-
timiza wajibu huo, lakini hata-
toa utumishi wowote. Utawafa-
nyia Walawi hivyo katika waji-
bu wao mbalimbali."[h]

SURA 8

a Law 1:4
Hes 3:9
b Hes 3:41
Hes 3:45
c Law 7:30
Law 8:27
Hes 8:21
d Hes 1:50
Hes 3:6
e Kut 29:10
f Law 1:4
g Hes 3:45
Hes 16:9
h Hes 4:3
Hes 8:11
i Kut 29:24
j Hes 3:45
k Hes 3:12
l Kut 13:2
Kut 13:12
Hes 3:13
Lu 2:23
m Kut 12:29
Zb 78:51
Zb 105:36
Zb 135:8
Ebr 11:28
n Kut 13:15
Law 27:26
o Hes 3:12

Safu ya 2

a Hes 3:9
Hes 18:6
b 1Nya 23:32
Eze 44:11
c Hes 1:53
Hes 18:5
1Sa 6:19
2Nya 26:16
d Hes 8:7
e Hes 8:11
f Hes 8:12
g Hes 8:15
2Nya 31:2
h Hes 1:53
Hes 3:32
Hes 18:4
1Nya 23:32
Eze 44:11

9 Na Yehova akasema na Musa katika nyika ya Sinai katika mwaka wa pili baada ya kuondoka kwao katika nchi ya Misri, katika mwezi wa kwanza,[a] na kumwambia: **2** "Sasa wana wa Israeli watatayarisha dhabihu ya pasaka[b] katika wakati wake uliowekwa.[c] **3** Katika siku ya kumi na nne ya mwezi huu katikati ya zile jioni mbili[d] mtaitayarisha katika wakati wake uliowekwa. Kulingana na sheria zake zote na utaratibu wake wote wa kawaida mtaitayarisha."[e]

4 Basi Musa akawaambia wana wa Israeli waitayarishe dhabihu ya pasaka. **5** Basi wakaitayarisha dhabihu ya pasaka katika mwezi wa kwanza, siku ya kumi na nne ya mwezi huo katikati ya zile jioni mbili, katika nyika ya Sinai. Kulingana na yote ambayo Yehova alikuwa amemwamuru Musa, ndivyo wana wa Israeli walivyofanya.[f]

6 Sasa kukawa na watu ambao walikuwa wamekuwa najisi kwa sababu ya nafsi[g] ya binadamu hivi kwamba hawakuweza kuitayarisha dhabihu ya pasaka katika siku hiyo. Kwa hiyo wakaenda mbele ya Musa na Haruni katika siku hiyo.[h] **7** Kisha watu hao wakamwambia: "Tumekuwa najisi kwa sababu ya nafsi ya binadamu. Kwa nini tuzuiwe kumtolea Yehova toleo[i] katika wakati wake uliowekwa katikati ya wana wa Israeli?" **8** Ndipo Musa akawaambia: "Simameni hapo, acheni nisikie jambo ambalo Yehova ataamuru juu yenu."[j]

9 Ndipo Yehova akasema na Musa, na kumwambia:

SURA 9
a Kut 40:2
Hes 1:1
b Kut 12:27
c Kut 12:6
Law 23:5
Hes 28:16
Kum 16:1
Yos 5:10
Mk 14:12
1Ko 5:7
d Kut 12:6
e Kut 12:8
f Kum 30:8
Mhu 12:13
g Law 21:11
Hes 5:2
Hes 6:6
Hes 19:14
Hes 19:16
h Kut 18:15
Hes 15:33
Hes 27:2
i Law 7:21
Kum 16:2
j Kut 25:22
Law 16:2
Zb 99:6

Safu ya 2
a Hes 5:2
b 2Nya 30:2
2Nya 30:15
c Kut 12:8
d Kut 12:10
e Kut 12:46
Zb 34:20
Yoh 19:36
f Kut 12:43
g Kut 12:15
h Yak 4:17
i Kut 12:19
Kut 12:48
j Kut 12:8
k Kut 12:49
Law 24:22
Kum 29:11
Kum 31:12
Ro 2:11
l Kut 40:2
Kut 40:17
m Kut 14:24
Kut 40:34
Ne 9:12
n Kut 13:21
Kut 40:38
Hes 14:14
o Kut 13:22
Kum 1:33
Ne 9:19

10 "Sema na wana wa Israeli, na kuwaambia, 'Ingawa huenda mtu yeyote kati yenu au wa vizazi vyenu akawa najisi kwa sababu ya nafsi[a] au ameenda safari ya mbali, yeye pia lazima atamtayarishia Yehova dhabihu ya pasaka. **11** Katika mwezi wa pili,[b] siku ya kumi na nne katikati ya zile jioni mbili, wataitayarisha. Wataila pamoja na keki zisizo na chachu na mboga chungu.[c] **12** Hawapaswi kuacha chochote mpaka asubuhi,[d] wala hawapaswi kuvunja mfupa wowote ulio ndani yake.[e] Wanapaswa kuitayarisha kulingana na sheria yote ya pasaka.[f] **13** Lakini wakati ambapo mtu alikuwa safi au hakuwa ameenda safari naye alipuuza kuitayarisha dhabihu ya pasaka, basi lazima nafsi hiyo itakatiliwa mbali kutoka kwa watu wake,[g] kwa sababu haikutoa toleo la Yehova katika wakati wake uliowekwa. Mtu huyo atajibu kwa sababu ya dhambi yake.[h]

14 "'Na ikiwa mkaaji mgeni atakuwa akikaa pamoja nanyi akiwa mgeni, yeye pia atamtayarishia Yehova dhabihu ya pasaka.[i] Anapaswa kufanya kulingana na sheria ya pasaka na kulingana na utaratibu wake wa kawaida.[j] Kutakuwa na sheria moja kwa ajili yenu, kwa ajili ya mkaaji mgeni na kwa ajili ya mwenyeji wa nchi.'"[k]

15 Sasa katika siku ya kusimamisha maskani[l] wingu lilifunika maskani ya hema la Ushuhuda,[m] lakini wakati wa jioni kitu kilichoonekana kama moto[n] kilikaa juu ya maskani hiyo mpaka asubuhi. **16** Hivyo ndivyo ilivyoendelea daima: Wingu liliifunika wakati wa mchana, na kitu kilichoonekana kama moto wakati wa usiku.[o] **17** Na

wakati wowote wingu hilo lilipoinuka kutoka juu ya hema, wana wa Israeli walikuwa wakiondoka mara moja baada yake,[a] na mahali ambapo wingu hilo lilikuwa likikaa, hapo ndipo wana wa Israeli walipokuwa wakipiga kambi.[b] **18** Wana wa Israeli walikuwa wakiondoka kwa agizo la Yehova, na kupiga kambi kwa agizo la Yehova.[c] Siku zote ambazo wingu hilo lilikaa juu ya maskani, walikaa katika kambi. **19** Na wakati ambapo wingu hilo lilirefusha kukaa kwake juu ya maskani hiyo siku nyingi, wana wa Israeli pia walishika wajibu wao kwa Yehova kwamba wasiondoke.[d] **20** Na nyakati fulani wingu hilo lilikaa siku chache juu ya maskani. Walikuwa wakipiga kambi kwa agizo[e] la Yehova, na kuondoka kwa agizo la Yehova. **21** Na nyakati fulani wingu[f] hilo lilikaa kuanzia jioni mpaka asubuhi; na wingu hilo liliondoka wakati wa asubuhi, nao wakaondoka. Iwe wingu hilo liliinuka mchana au usiku, wao pia waliondoka.[g] **22** Iwe wingu hilo lilirefusha kukaa kwake juu ya maskani kwa siku mbili au mwezi au siku zaidi, wana wa Israeli waliendelea kukaa katika kambi nao hawakuwa wakiondoka, lakini lilipoinuka waliondoka.[h] **23** Walipiga kambi kwa agizo la Yehova, na kuondoka kwa agizo la Yehova. Walishika wajibu[i] wao kwa Yehova kufuatia agizo la Yehova kupitia Musa.[j]

10 Na Yehova akasema na Musa, na kumwambia: **2** "Jifanyie tarumbeta[k] mbili za fedha. Utazifua, nawe utazitumia kuliita[l] kusanyiko na kwa ajili ya kuzivunja kambi. **3** Nao watazipiga zote mbili, nalo kusanyiko lote litakutana nawe kwenye mwingilio wa hema la mkutano.[a] **4** Na ikiwa watapiga moja tu, ndipo wakuu wakiwa vichwa vya maelfu ya Israeli watakutana nawe kama ilivyopangwa.[b]

5 "Nanyi mtapiga mvumo unaopanda na kushuka, nazo kambi za wale wanaopiga kambi upande wa mashariki[c] zitaondoka. **6** Nanyi mtapiga mvumo unaopanda na kushuka kwa mara ya pili, nazo kambi za wale wanaopiga kambi upande wa kusini[d] zitaondoka. Watapiga mvumo unaopanda na kushuka kila mara moja kati yazo inapoondoka.

7 "Sasa wakati wa kuita kutaniko pamoja, mtapiga,[e] lakini hamtapiga mvumo unaopanda na kushuka. **8** Nao wana wa Haruni, kuhani, watazipiga tarumbeta,[f] nazo zitakuwa sheria kwa ajili yenu mpaka wakati usio na kipimo katika vizazi vyenu.

9 "Na ikiwa mtaingia vitani katika nchi yenu kupigana na mkandamizaji anayewasumbua ninyi,[g] mnapaswa pia kutoa mwito wa vita kwa tarumbeta[h] nanyi hakika mtakumbukwa mbele za Yehova Mungu wenu na kuokolewa kutoka kwa adui zenu.[i]

10 "Na katika siku ya kushangilia[j] kwenu na katika majira yenu ya sherehe[k] na mwanzoni mwa miezi yenu,[l] mtapiga tarumbeta juu ya matoleo yenu ya kuteketezwa[m] na dhabihu zenu za ushirika;[n] nazo zitakuwa ukumbusho kwa ajili yenu mbele za Yehova Mungu wenu. Mimi ni Yehova Mungu wenu."[o]

11 Sasa ikawa kwamba kati-

SURA 9

a Kut 40:36
Hes 10:11
Hes 10:34
b Kut 33:14
Kut 40:37
c Kut 17:1
Hes 10:13
d Kut 40:37
Hes 1:52
e Zb 48:14
f Zb 78:14
g Kut 40:36
Hes 9:17
h Kum 1:7
Kum 2:3
i Kut 24:3
Hes 9:19
Kum 11:1
Yos 22:3
j Kut 39:42

SURA 10

k Law 23:24
Law 25:9
l Zb 81:3
Yoe 1:14

Safu ya 2

a Hes 1:18
Kum 29:10
Yer 4:5
b Kut 18:21
Hes 1:16
Hes 7:2
Kum 1:15
Kum 5:23
Kum 31:9
c Hes 2:3
d Hes 2:10
e Hes 10:3
Yoe 2:15
f Hes 31:6
1Nya 15:24
1Nya 16:6
2Nya 29:26
Ne 12:35
Ne 12:41
g Amu 2:18
Amu 6:9
h Amu 3:27
Amu 7:20
2Nya 13:12
1Ko 14:8
i Zb 106:4
j 1Nya 15:28
2Nya 5:12
2Nya 7:6
Ezr 3:10
k Law 23:24
Hes 29:1
l Zb 81:3
m Hes 28:11
n Law 3:1
Hes 29:39
o Kut 6:7
Law 11:45

ka mwaka wa pili, katika mwezi
wa pili, siku ya 20 katika mwe-
zi huo,[a] lile wingu likainuka ku-
toka juu ya maskani[b] ya Ushu-
huda. **12** Nao wana wa Israeli
wakaanza kuondoka katika na-
mna ya kuondoka[c] kwao kuto-
ka katika nyika ya Sinai, nalo
wingu likakaa katika nyika
ya Parani.[d] **13** Nao wakaanza
kuondoka kwa mara ya kwa-
nza, kulingana na agizo la Yeho-
va kupitia Musa.[e]

14 Kwa hiyo ule mgawanyo
wa makabila matatu wa kambi
ya wana wa Yuda ndio ulioondo-
ka kwanza kabisa, kwa majeshi
yao,[f] naye Nashoni[g] mwana wa
Aminadabu alikuwa juu ya je-
shi la mgawanyo huo. **15** Na
juu ya jeshi la kabila la wana wa
Isakari kulikuwa na Nethaneli[h]
mwana wa Zuari. **16** Na juu ya
jeshi la kabila la wana wa Zabu-
loni kulikuwa na Eliabu mwana
wa Heloni.[i]

17 Nayo maskani ikashu-
shwa,[j] nao wana wa Gershoni[k]
na wana wa Merari,[l] wakiwa
wachukuzi wa maskani wakao-
ndoka.

18 Nao ule mgawanyo wa ma-
kabila matatu wa kambi ya Ru-
beni[m] ukaondoka, kwa majeshi
yao, naye Elisuri[n] mwana wa
Shedeuri alikuwa juu ya jeshi
lake. **19** Na juu ya jeshi la ka-
bila la wana wa Simeoni[o] kuli-
kuwa na Shelumieli[p] mwana wa
Zurishadai. **20** Na juu ya jeshi
la kabila la wana wa Gadi ku-
likuwa na Eliasafu[q] mwana wa
Deueli.

21 Nao Wakohathi wakiwa
wachukuzi wa patakatifu[r] wa-
kaondoka, kwa maana watuku-
wa wameisimamisha maskani
kufikia wakati wa kuja kwao.

22 Na ule mgawanyo wa ma-
kabila matatu wa kambi ya
wana wa Efraimu[a] ukaondoka,
kwa majeshi yao, naye Elisha-
ma[b] mwana wa Amihudi aliku-
wa juu ya jeshi lake. **23** Na juu
ya jeshi la kabila la wana wa
Manase[c] kulikuwa na Gamalie-
li[d] mwana wa Pedazuri. **24** Na
juu ya jeshi la kabila la wana wa
Benyamini[e] kulikuwa na Abida-
ni[f] mwana wa Gidioni.

25 Na ule mgawanyo wa ma-
kabila matatu wa kambi ya
wana wa Dani[g] ukaondoka uki-
fanyiza kikosi cha nyuma cha
ulinzi[h] kwa ajili ya kambi zote,
kwa majeshi yao, naye Ahiezeri[i]
mwana wa Amishadai alikuwa
juu ya jeshi lake. **26** Na juu ya
jeshi la kabila la wana wa Ashe-
ri[j] kulikuwa na Pagieli[k] mwa-
na wa Okrani. **27** Na juu ya je-
shi la kabila la wana wa Naftali[l]
kulikuwa na Ahira[m] mwana wa
Enani. **28** Hivyo ndivyo wana
wa Israeli walivyoondoka, kwa
majeshi yao, walipokuwa wakio-
ndoka.[n]

29 Ndipo Musa akamwa-
mbia Hobabu mwana wa Reue-
li[o] Mmidiani, baba-mkwe wa
Musa: "Tunaondoka kwenda
mahali ambapo Yehova alise-
ma, 'Nitawapa ninyi.'[p] Nenda
pamoja nasi, nasi hakika tu-
takutendea mema,[q] kwa saba-
bu Yehova amesema mema juu
ya Israeli."[r] **30** Lakini aka-
mwambia: "Sitaenda pamoja
nanyi, bali nitaenda katika nchi
yangu[s] mwenyewe na kwa ja-
maa zangu." **31** Basi akase-
ma: "Tafadhali, usituache, kwa
sababu unajua vema mahali
ambapo tunaweza kupiga ka-
mbi nyikani, utakuwa macho
yetu. **32** Na itakuwa kwamba
ikiwa utaenda pamoja nasi,[t]
naam, itakuwa kwamba wema

SURA 10

a Hes 1:1
b Hes 9:17
Zb 78:14
c Kut 40:36
Hes 2:9
Hes 2:16
Hes 2:17
Hes 2:24
Hes 2:31
d Mwa 21:21
Hes 12:16
Hes 13:26
Kum 1:2
e Hes 2:34
Hes 9:23
f Hes 2:3
g Hes 1:7
h Hes 1:8
Hes 2:5
i Hes 2:7
j Hes 1:51
k Hes 3:25
l Hes 3:36
m Hes 2:10
n Hes 1:5
o Hes 2:12
p Hes 1:6
q Hes 1:14
Hes 2:14
r Hes 3:31
Hes 4:4
Hes 4:15
Hes 7:9

Safu ya 2

a Hes 2:24
b Hes 1:10
Hes 2:18
c Hes 2:20
d Hes 1:10
e Hes 2:22
f Hes 1:11
g Hes 2:25
Hes 2:31
h Yos 6:9
i Hes 1:12
j Hes 2:27
k Hes 1:13
l Hes 2:29
m Hes 1:15
n Hes 2:34
o Kut 2:18
Kut 3:1
Kut 18:1
Kut 18:27
p Mwa 12:7
Mwa 13:15
Mwa 15:18
Mdo 7:5
q Amu 1:16
Amu 4:11
1Sa 15:6
r Mwa 32:12
Kut 3:8
Kut 6:7
Hes 23:19
s Kut 3:1
t Amu 1:16
Amu 4:11

ambao Yehova atatutendea, sisi nasi tutakutendea wewe."

33 Kwa hiyo wakapiga mwendo kutoka mlima wa Yehova[a] safari ya siku tatu, nalo sanduku la agano[b] la Yehova lilikuwa likipiga mwendo mbele yao kwa safari ya siku tatu ili kutafuta mahali pa kupumzika kwa ajili yao.[c] **34** Nalo wingu[d] la Yehova lilikuwa juu yao wakati wa mchana walipokuwa wakipiga mwendo kutoka katika kambi.

35 Na ikawa kwamba Sanduku lilipokuwa likiondoka, Musa alikuwa akisema: "Usimame, Ee Yehova, adui zako na watawanyike;[e] na wale wanaokuchukia vikali wakimbie toka mbele zako."[f] **36** Na lilipopumzika, alikuwa akisema: "Urudi, Ee Yehova, kwa makumi ya maelfu ya maelfu ya Israeli."[g]

11 Sasa watu wakawa kama watu wenye jambo baya la kulalamika masikioni mwa Yehova.[h] Yehova alipolisikia jambo hilo, hasira yake ikawaka, nao moto wa Yehova ukaanza kuwaka juu yao na kuteketeza wengine kati yao katika mwisho wa kambi.[i] **2** Watu walipoanza kumlilia Musa, ndipo yeye akamwomba Yehova dua,[j] nao moto ukapoa. **3** Na jina la mahali hapo likaitwa Tabera,[k] kwa sababu moto wa Yehova ulikuwa umewaka juu yao.

4 Nao umati uliochangamana[l] uliokuwa katikati yao ukaonyesha tamaa ya uchoyo,[m] na wana wa Israeli pia wakaanza kulia tena na kusema: "Ni nani atakayetupa nyama tule?[n] **5** Jinsi tunavyokumbuka samaki tuliokuwa tukila bure huko Misri,[o] matango na matikiti-maji na vitunguu vya majani na vitunguu na vitunguu saumu! **6** Lakini sasa nafsi yetu imekauka. Macho yetu hayaoni chochote isipokuwa mana."[a]

7 Mana[b] ilikuwa kama mbegu ya mgiligilani[c] nayo ilionekana kama ulimbo wa bedola.[d] **8** Watu walitawanyika na kuiokota[e] na kuisaga katika mawe ya kusaga ya mkononi au kuitwanga katika kinu, nao waliitokosa katika vyungu vya kupikia[f] au kuifanya kuwa keki za mviringo, nayo ladha yake ilikuwa kama ladha ya keki tamu iliyotiwa mafuta.[g] **9** Na umande uliposhuka juu ya kambi usiku, mana ilishuka juu yake.[h]

10 Na Musa akawasikia watu wakilia katika familia zao, kila mtu kwenye mwingilio wa hema lake. Na hasira ya Yehova ikaanza kuwaka sana,[i] na machoni pa Musa lilikuwa jambo baya.[j] **11** Ndipo Musa akamwambia Yehova: "Kwa nini umemsababishia mtumishi wako uovu, na kwa nini sijapata kibali machoni pako, kwa kuuweka mzigo wa watu wote hawa juu yangu?[k] **12** Je, nilichukua mimba ya watu hawa wote? Je, ni mimi niliyewazaa, hivi kwamba uniambie, 'Wabebe kifuani pako,[l] kama vile mwanamume mlezi anavyombeba mtoto anayenyonya,'[m] mpaka katika nchi uliyowaapia mababu zao?[n] **13** Nitatoa wapi nyama ya kuwapa watu wote hawa? Kwa maana wananililia daima, na kusema, 'Tupe nyama, tule!' **14** Mimi siwezi, mimi peke yangu, kuwabeba watu wote hawa, kwa sababu ni wazito mno kwangu.[o] **15** Kwa hiyo ikiwa hivi ndivyo unavyonifanyia, tafadhali niue kabisa,[p] ikiwa nimepata kibali

SURA 10
a Kut 3:1; Kut 19:3; Kut 24:16; Kum 5:2; 1Fa 19:8; Mal 4:4
b Kut 25:10; Kut 25:17
c Kum 1:33; Yos 3:3; Yos 3:4
d Kut 13:21; Ne 9:12; Zb 78:14; Zb 105:39
e Zb 17:13; Zb 132:8
f Zb 68:1
g Kum 1:10

SURA 11
h Kum 9:22
i Zb 78:21; Zb 106:18
j Kut 32:11; Kum 9:19; Zb 106:23; Yak 5:16
k Kum 9:22
l Kut 12:38; Law 24:10
m 1Ko 10:10
n Zb 78:18; Zb 78:22; Zb 106:14
o Kut 16:3

Safu ya 2
a Kut 16:35; Hes 21:5
b Kut 16:14; Ne 9:20; Yoh 6:31; Yoh 6:33; Yoh 6:51
c Kut 16:31
d Mwa 2:12
e Kut 16:16
f Kut 16:23
g Kut 16:31
h Zb 78:24
i Hes 11:1; Kum 32:22; Zb 78:21
j Met 29:27
k Kut 17:4; Kum 1:12
l Isa 40:11
m 1Th 2:7
n Mwa 13:15; Mwa 26:3; Mwa 50:24; Kut 13:5
o Kut 18:18; Kum 1:9
p 1Fa 19:4; Ayu 6:9

machoni pako, wala usiache niutazame msiba wangu."

16 Basi Yehova akamwambia Musa: "Nikusanyie wanaume 70 kati ya wanaume wazee wa Israeli,[a] ambao unajua kwamba ni wanaume wazee wa watu na maofisa wao,[b] nawe utawapeleka kwenye hema la mkutano, nao watasimama hapo pamoja nawe. **17** Nami nitashuka chini[c] na kusema nawe huko;[d] nami nitaondoa sehemu ya roho[e] iliyo juu yako na kuiweka juu yao, nao watakusaidia kuubeba mzigo wa watu ili usiubebe, wewe peke yako.[f] **18** Nawe utawaambia watu hao, 'Jitakaseni kwa ajili ya kesho,[g] kwa maana hakika mtakula nyama, kwa sababu mmelia masikioni mwa Yehova,[h] na kusema: "Ni nani atakayetupa nyama tule, kwa maana mambo yalituendea vema huko Misri?"[i] Na Yehova hakika atawapa nyama, nanyi kwa kweli mtakula.[j] **19** Mtakula, si siku moja wala siku 2 wala siku 5 wala siku 10 wala siku 20, **20** bali mwezi mzima, mpaka itokee kwenye mianzi ya pua zenu nayo iwe chukizo kwenu,[k] kwa sababu tu mlimkataa Yehova, aliye katikati yenu, nanyi mlilia mbele zake, na kusema: "Kwa nini tumetoka Misri?""[l]

21 Ndipo Musa akasema: "Watu nilio katikati yao ni wanaume mia sita elfu[m] wanaotembea kwa miguu, hata hivyo wewe—wewe umesema, 'Nitawapa nyama, nao hakika watakula kwa mwezi mzima'! **22** Je, mifugo na makundi yatachinjwa kwa ajili yao, ili iwatoshe?[n] Au samaki wote wa baharini watakamatwa kwa ajili yao, ili iwatoshe?"

SURA 11

a Kut 24:1
Kut 24:9
b Kum 16:18
c Mwa 17:22
Kut 19:11
Kut 25:22
Kut 34:5
Hes 12:5
d Hes 11:25
Hes 12:8
e Hes 27:18
1Sa 10:6
2Fa 2:15
Ne 9:20
Mdo 2:17
f Kut 18:22
g Kut 19:10
h Kut 16:7
i Hes 11:4
Hes 11:5
j Kut 16:8
k Zb 78:29
Zb 106:15
l Hes 21:5
m Mwa 12:2
Kut 12:37
Kut 38:26
Hes 1:46
n Mt 15:33

Safu ya 2

a Mwa 18:14
Isa 50:2
Isa 59:1
Mk 10:27
Lu 1:37
b Isa 55:11
Yer 44:28
Tit 1:2
Ebr 6:18
c Hes 11:16
d Kut 33:9
Hes 12:5
Kum 31:15
e Zb 99:7
f Hes 11:17
2Fa 2:9
2Fa 2:15
g 1Sa 10:6
1Sa 19:20
h Kut 17:9
Kut 24:13
Kut 33:11
Hes 27:18
Kum 31:3
i Mk 9:38
j Yoe 2:28
Mdo 26:29

23 Ndipo Yehova akamwambia Musa: "Je, mkono wa Yehova ni mfupi?[a] Sasa utaona ikiwa ninalosema litatukia kwako au hapana."[b]

24 Kisha Musa akatoka na kusema na watu maneno ya Yehova. Naye akakusanya wanaume 70 kutoka kwa wanaume wazee wa watu na kuwasimamisha kulizunguka hema pande zote.[c] **25** Ndipo Yehova akashuka katika wingu,[d] akasema naye,[e] akachukua sehemu ya roho[f] iliyokuwa juu yake na kuiweka juu ya kila mmoja wa wale wanaume wazee 70. Na ikawa kwamba mara tu roho hiyo ilipotua juu yao, ndipo wakaanza kutenda kama manabii; lakini hawakufanya hivyo tena.[g]

26 Sasa kulikuwa na wawili kati ya wanaume hao waliobaki katika kambi. Jina la mmoja wao lilikuwa Eldadi, na jina la yule mwingine lilikuwa Medadi. Nayo roho ikaanza kushuka juu yao, kwa maana walikuwa kati ya wale walioandikwa, lakini hawakuwa wameenda kwenye hema. Basi wakaanza kutenda kama manabii katika kambi. **27** Na mwanamume mmoja kijana akakimbia na kumletea Musa habari na kusema: "Eldadi na Medadi wanatenda kama manabii katika kambi!" **28** Ndipo Yoshua mwana wa Nuni, mhudumu[h] wa Musa tangu ujana wake, akajibu na kusema: "Bwana wangu Musa, wazuie!"[i] **29** Hata hivyo, Musa akamwambia: "Je, unaona wivu kwa ajili yangu? Hapana, laiti watu wote wa Yehova wangekuwa manabii, kwa sababu Yehova angeiweka roho yake juu yao!"[j] **30** Baadaye

Musa akaondoka, akaenda kambini, yeye na wale wanaume wazee wa Israeli.

31 Na upepo[a] ukavuma kutoka kwa Yehova na kuanza kusukuma kware kutoka baharini[b] na kuwaangusha juu ya kambi karibu safari ya siku moja kwenda upande huu na karibu safari ya siku moja kwenda upande ule, pande zote kuizunguka kambi, na karibu kimo cha mikono miwili juu ya uso wa dunia. **32** Ndipo watu wakasimama siku hiyo mchana kutwa na usiku kucha na kesho yake mchana kutwa nao wakaendelea kuokota kware. Yeye aliyeokota kidogo zaidi alikusanya homeri[c] kumi, nao wakawatandaza katika eneo kubwa pande zote za kambi kwa ajili yao. **33** Nyama hiyo ilikuwa ingali bado katikati ya meno yao,[d] kabla haijatafunwa, wakati hasira ya Yehova ilipowaka[e] juu ya watu hao, na Yehova akaanza kuwapiga watu kwa mauaji makubwa sana.[f]

34 Jina la mahali hapo likaitwa Kibroth-hataava,[g] kwa sababu hapo waliwazika watu walioonyesha tamaa ya uchoyo.[h] **35** Kutoka Kibroth-hataava watu wakafunga safari kuelekea Haserothi, nao wakaendelea kukaa Haserothi.[i]

12 Sasa Miriamu na Haruni wakaanza kusema dhidi ya Musa kwa sababu ya mke Mkushi ambaye alikuwa amemchukua, kwa sababu alikuwa amemchukua mke Mkushi.[j] **2** Nao wakawa wakisema: "Je, Yehova amesema kupitia Musa tu? Je, hajasema kupitia sisi pia?"[k] Na Yehova alikuwa akisikiliza.[l] **3** Naye mtu huyu Musa alikuwa mpole[a] zaidi kuliko watu wote waliokuwa juu ya uso wa nchi.

4 Ndipo ghafula Yehova akawaambia Musa na Haruni na Miriamu: "Tokeni, ninyi watatu, mwende kwenye hema la mkutano." Basi hao watatu wakatoka. **5** Kisha Yehova akashuka katika nguzo ya wingu[b] na kusimama kwenye mwingilio wa hema na kuwaita Haruni na Miriamu. Nao wakaenda nje. **6** Naye akasema: "Sikieni maneno yangu, tafadhali. Kungalikuwa na nabii kati yenu kwa ajili ya Yehova, ningalijijulisha kwake katika maono.[c] Ningalisema naye katika ndoto.[d] **7** Sivyo ilivyo kwa mtumishi wangu Musa![e] Amekabidhiwa nyumba yangu yote.[f] **8** Mimi husema naye kinywa kwa kinywa,[g] na hivyo kumwonyesha, wala si kwa vitendawili;[h] naye huona sura ya Yehova.[i] Kwa nini, basi, hamkuogopa kusema juu ya mtumishi wangu, juu ya Musa?"[j]

9 Nayo hasira ya Yehova ikawaka juu yao, naye akaenda zake. **10** Nalo wingu likageuka na kutoka juu ya hema, na, tazama! Miriamu alikuwa amepigwa kwa ukoma mweupe kama theluji.[k] Ndipo Haruni akageuka kumwelekea Miriamu, na, tazama! alikuwa amepigwa kwa ukoma.[l] **11** Mara moja Haruni akamwambia Musa: "Nakuomba radhi, bwana wangu! Tafadhali, usituhesabie dhambi ambayo tumetenda kwa upumbavu na ambayo tumefanya![m] **12** Tafadhali, usimwache aendelee kuwa kama mtu aliyekufa,[n] ambaye nyama yake wakati wa kutoka kwake katika tumbo la uza-

SURA 11
a Zb 78:26
Zb 135:7
b Kut 16:13
Zb 78:27
Zb 105:40
c Kut 16:36
Eze 45:11
d Zb 78:30
Zb 106:15
e Zb 78:31
f 1Ko 10:10
g Hes 33:16
Kum 9:22
h 1Ko 10:6
i Hes 33:17
Kum 1:1

SURA 12
j Kut 2:16
Kut 2:21
k Kut 4:15
Kut 4:30
Kut 15:20
Kut 28:30
Mik 6:4
l Hes 11:1
2Fa 19:4

Safu ya 2
a Zb 147:6
Zb 149:4
Mt 11:29
Mt 21:5
1Pe 3:4
b Kut 34:5
Hes 11:25
Zb 99:7
c Mwa 15:1
Mwa 46:2
Kut 24:11
Ayu 33:15
d Mwa 31:10
Yer 23:28
e Zb 105:26
f Ebr 3:2
g Kut 33:11
Kum 34:10
h Zb 49:4
1Ko 13:12
i Kut 24:10
j Kut 34:30
2Pe 2:10
Yud 8
k Kum 24:9
l 2Nya 26:19
m 2Sa 24:10
Met 30:32
Mk 7:20
n Law 13:45

zi la mama yake imeliwa nusu!”
13 Na Musa akaanza kumlilia
Yehova, na kusema: “Ee Mu-
ngu, tafadhali! Mponye, tafa-
dhali!”[a]

14 Ndipo Yehova akamwa-
mbia Musa: “Ikiwa baba yake
angemtemea mate[b] moja kwa
moja usoni pake, je, hangefe-
dheheshwa siku saba? Na ate-
ngwe[c] siku saba nje ya kambi,[d]
kisha apokewe ndani baada-
ye.”[e] **15** Kwa hiyo Miriamu
akatengwa nje ya kambi siku
saba,[f] nao watu hawakuondo-
ka mpaka Miriamu alipopoke-
wa ndani. **16** Kisha watu wa-
kaondoka Haserothi[g] na kupiga
kambi katika nyika ya Parani.[h]

13 Sasa Yehova akasema na
Musa, na kumwambia:
2 “Tuma watu kwa ajili yako
wapate kuipeleleza nchi ya Ka-
naani, ninayowapa wana wa
Israeli.[i] Mtamtuma mtu mmo-
ja kwa ajili ya kila kabila
la baba yake, kila mmoja wao
mkuu[j] kati yao.”

3 Basi Musa akawatuma kuto-
ka katika nyika ya Parani[k] kwa
agizo la Yehova. Wanaume wote
hao walikuwa vichwa vya wana
wa Israeli. **4** Na haya ndiyo
majina yao: Wa kabila la Rube-
ni, Shamua mwana wa Zakuri;
5 wa kabila la Simeoni, Shafa-
ti mwana wa Hori; **6** wa kabila
la Yuda, Kalebu[l] mwana wa Yefu-
ne; **7** wa kabila la Isakari, Iga-
li mwana wa Yosefu; **8** wa ka-
bila la Efraimu, Hoshea[m] mwa-
na wa Nuni; **9** wa kabila la Be-
nyamini, Palti mwana wa Rafu;
10 wa kabila la Zabuloni, Gadie-
li mwana wa Sodi; **11** wa kabi-
la la Yosefu,[n] kwa ajili ya kabila
la Manase,[o] Gadi mwana wa Susi;
12 wa kabila la Dani, Amieli
mwana wa Gemali; **13** wa kabi-
la la Asheri, Sethuri mwana wa
Mikaeli; **14** wa kabila la Naf-
tali, Nabi mwana wa Vofsi;
15 wa kabila la Gadi, Geueli
mwana wa Maki. **16** Hayo ndi-
yo majina ya wanaume ambao
Musa aliwatuma wakaipeleleze
nchi. Na huyo Hoshea mwa-
na wa Nuni, Musa akamwita Ye-
hoshua.[a]

17 Musa alipokuwa akiwatu-
ma kuipeleleza nchi ya Kanaa-
ni, aliwaambia: “Pandeni hapa
na kuingia Negebu,[b] nanyi mta-
panda na kuingia katika eneo
lenye milima.[c] **18** Nanyi mta-
ona jinsi nchi ilivyo[d] na watu
wanaokaa humo, ikiwa wana
nguvu au ni dhaifu, ikiwa ni
wachache au ni wengi; **19** na
jinsi nchi wanayokaa ndani
yake ilivyo, iwapo ni nzuri au
ni mbaya, na jinsi majiji wana-
yokaa ndani yake yalivyo, iwa-
po ni katika kambi au ni kati-
ka ngome; **20** Na jinsi nchi ili-
vyo, iwapo ni nono au imeko-
nda,[e] iwapo kuna miti ndani
yake au hakuna. Nanyi mjio-
nyeshe kuwa hodari[f] na kuchu-
kua baadhi ya matunda ya nchi
hiyo.” Sasa siku hizo zilikuwa
siku za matunda yaliyoiva ya
kwanza ya zabibu.[g]

21 Basi wakapanda na kui-
peleleza nchi kutoka katika
nyika ya Zini[h] mpaka Rehobu[i]
mpaka mahali pa kuingi-
lia pa Hamathi.[j] **22** Walipopa-
nda kuingia Negebu,[k] ndipo wa-
kafika Hebroni.[l] Sasa Ahimani,
Sheshai na Talmai,[m] wale wa-
liozaliwa kwa Anaki[n] walikuwa
huko. Hebroni[o] lilikuwa li-
mejengwa miaka saba kabla ya
Soani[p] la Misri. **23** Walipofika
kwenye bonde la mto la Eshko-
li,[q] wakakata chipukizi lenye

SURA 12
a Kut 32:11
Yak 5:16
b Ayu 30:10
Isa 50:6
c Law 13:4
d Law 13:46
Hes 5:2
e Law 14:9
f Kum 24:9
g Hes 11:35
Hes 33:18
Kum 1:1
h Hes 10:12
Hes 13:26

SURA 13
i Hes 32:8
Kum 1:22
j Kut 18:25
Kum 1:15
k Hes 12:16
Kum 1:19
l Hes 13:30
Hes 14:30
Hes 14:38
Hes 34:19
1Nya 4:15
m Hes 11:28
Hes 13:16
Hes 14:30
Hes 34:17
n Mwa 48:5
o Mwa 48:19

Safu ya 2
a Kut 17:9
b Mwa 20:1
c Kum 1:7
Amu 1:9
d Kut 3:8
Kum 8:7
e Ne 9:25
Ne 9:35
Eze 20:6
f Kum 31:6
Yos 1:6
g Hes 13:23
h Hes 34:3
Yos 15:1
i 2Sa 10:6
2Sa 10:8
j Hes 34:8
Yos 13:5
Amo 6:2
k Hes 13:17
l Mwa 13:18
m Amu 1:10
n Kum 9:2
Yos 11:21
Yos 15:13
o Yos 21:11
p Zb 78:12
Isa 19:11
q Hes 32:9

kishada kimoja cha zabibu.[a] Na
wawili kati ya wanaume hao
wakalichukua kwa ufito, na pia
baadhi ya makomamanga[b] na
baadhi ya tini. **24** Wakapai-
ta mahali hapo bonde la mto la
Eshkoli,[c] kwa sababu ya kile ki-
shada ambacho wana wa Israe-
eli walikata kutoka huko.

25 Mwishowe, mwishoni
mwa siku 40[d] wakarudi kutoka
kuipeleleza nchi. **26** Basi wa-
katembea na kuja kwa Musa
na Haruni na kusanyiko lote
la wana wa Israeli katika nyika
ya Parani, huko Kadeshi.[e] Nao
wakaleta neno kwao na kwa
kusanyiko lote na kuwaonye-
sha matunda ya nchi. **27** Nao
wakampa habari na kusema:
"Tuliingia katika nchi uliyotu-
tuma, nayo kwa kweli inatiri-
rika maziwa na asali,[f] na haya
ni matunda yake.[g] **28** Hata
hivyo, mambo ya hakika ni
kwamba watu wanaokaa ka-
tika nchi hiyo ni wenye ngu-
vu, na majiji yenye ngome ni
makubwa sana;[h] na, pia, wa-
zao wa Anaki tuliwaona huko.[i]
29 Waamaleki[j] wanakaa katika
nchi ya Negebu,[k] na Wahiti na
Wayebusi[l] na Waamori[m] wana-
kaa katika eneo lenye milima,
na Wakanaani[n] wanakaa kando
ya bahari na kando ya ukingo
wa Yordani."

30 Ndipo Kalebu[o] akajari-
bu kuwatuliza watu mbele ya
Musa naye akasema: "Na tupa-
nde moja kwa moja, nasi tutai-
miliki, kwa sababu kwa hakika
tunaweza kuishinda."[p] **31** La-
kini wale watu waliopanda pa-
moja naye wakasema: "Hatuwe-
zi kupanda kupigana na watu
hao, kwa sababu ni wenye ngu-
vu kuliko sisi."[q] **32** Nao wa-
kazidi kuwaletea wana wa Isra-
eli habari mbaya[a] juu ya nchi
waliyokuwa wameipeleleza, na
kusema: "Ile nchi, tuliyoipitia
ili kuipeleleza, ni nchi ambayo
inakula wakaaji wake; na watu
wote tuliowaona katikati yake
ni watu wenye ukubwa usio wa
kawaida.[b] **33** Na humo tuli-
waona Wanefili, wana wa Ana-
ki,[c] waliotoka kwa Wanefili;
hivi kwamba sisi tukawa ma-
choni petu wenyewe kama pa-
nzi, na machoni pao sisi tukawa
vivyo hivyo."[d]

14 Ndipo kusanyiko lote li-
kapaaza sauti zao, nao
watu wakazidi kupaaza sau-
ti zao na kulia[e] usiku kucha.
2 Na wana wote wa Israeli wa-
kaanza kunung'unika juu ya
Musa na Haruni,[f] na kusanyiko
lote likaanza kusema dhidi yao:
"Laiti tungalikufa katika nchi
ya Misri, au laiti tungalikufa
katika nyika hii! **3** Na kwa
nini Yehova anatuleta kwe-
nye nchi hii ili tuanguke kwa
upanga?[g] Wake zetu na wato-
to wetu wadogo watakuwa nya-
ra.[h] Je, si afadhali kwetu turudi
Misri?"[i] **4** Hata wakaambia-
na: "Na tuchague kiongozi, nasi
turudi Misri!"[j]

5 Ndipo Musa na Haruni wa-
kaanguka kifudifudi[k] mbele
ya kutaniko lote la kusanyiko
la wana wa Israeli. **6** Na Yo-
shua mwana wa Nuni[l] na Kale-
bu mwana wa Yefune,[m] ambao
ni kati ya wale walioipeleleza
nchi hiyo, wakayararua mavazi
yao,[n] **7** nao wakaliambia ku-
sanyiko lote la wana wa Israeli
hivi: "Nchi tuliyoipitia ili kuipe-
leleza ni nchi nzuri sana, sana.[o]
8 Ikiwa Yehova amependezwa
nasi,[p] basi kwa hakika atatuin-
giza katika nchi hii na kutu-

SURA 13
a Kum 1:25
b Kum 8:8
c Kum 1:24
d Hes 14:34
e Kum 1:19
Yos 14:6
Zb 29:8
f Kut 3:8
Law 20:24
g Kum 1:25
h Kum 1:28
i Hes 13:22
Hes 13:33
j Mwa 36:12
Kut 17:8
1Sa 15:3
k Hes 13:17
l Mwa 10:16
Kut 23:23
Kum 7:1
Amu 1:21
2Sa 5:8
m Yos 3:10
n Mwa 10:19
Kum 20:17
o Hes 14:6
p Yos 14:7
Zb 60:12
q Hes 32:9
Kum 1:28
Yos 14:8

Safu ya 2
a Hes 14:36
Hes 32:9
b Amo 2:9
c Kum 1:28
Kum 9:2
d Kum 2:10

SURA 14
e Kum 1:32
f Kum 1:27
Zb 106:25
g Hes 14:29
Zb 78:40
h Hes 14:31
Kum 1:39
i Hes 11:5
j Kum 1:34
Ne 9:17
Ebr 10:38
k Kum 9:26
l Hes 13:8
Hes 13:16
m Hes 13:6
Hes 14:30
n Yos 7:6
o Hes 13:27
Kum 1:25
Kum 8:7
Kum 11:14
p Kum 9:5
Kum 10:15

pa sisi, nchi inayotiririka maziwa na asali.[a] **9** Ila tu msimwasi Yehova;[b] nanyi msiwaogope watu wa nchi hiyo,[c] kwa maana wao ni mkate kwetu. Ulinzi wao umegeuka kutoka juu yao,[d] na Yehova yuko pamoja nasi.[e] Msiwaogope."[f]

10 Hata hivyo, kusanyiko lote likasema wapigwe kwa mawe.[g] Na utukufu wa Yehova ukaonekana juu ya hema la mkutano machoni pa wana wote wa Israeli.[h]

11 Mwishowe Yehova akamwambia Musa: "Watu hawa wataendelea kunitendea bila heshima[i] mpaka wakati gani,[j] nao watakosa kuniamini mpaka wakati gani ijapokuwa ishara zote ambazo nilifanya katikati yao?[k] **12** Acha niwapige kwa tauni na kuwafukuzia mbali, na acha nikufanye wewe kuwa taifa kubwa zaidi na lenye nguvu zaidi kuliko wao."[l]

13 Lakini Musa akamwambia Yehova: "Ndipo hakika Wamisri watasikia kwamba kwa nguvu zako uliwaongoza watu hawa kutoka katikati yao.[m] **14** Nao hakika watawaambia wakaaji wa nchi hii. Wamesikia kwamba wewe ni Yehova katikati ya watu hawa,[n] ambaye umeonekana uso kwa uso.[o] Wewe ni Yehova, nalo wingu lako linasimama juu yao, nawe unaenda mbele yao katika nguzo ya wingu wakati wa mchana na katika nguzo ya moto wakati wa usiku.[p] **15** Ukiwaua watu hawa kama mtu mmoja,[q] ndipo mataifa ambayo yamesikia juu ya sifa yako watasema hivi, **16** 'Kwa sababu Yehova hakuweza kuwaleta watu hawa katika nchi ambayo aliwaapia, aliwaua nyikani.'[r] **17** Na sasa, tafadhali, nguvu zako na ziwe kuu,[a] Ee Yehova, kama ulivyonena, na kusema, **18** 'Yehova, si mwepesi wa hasira[b] na ni mwingi wa fadhili zenye upendo,[c] anayesamehe kosa na ubaya,[d] lakini ambaye kwa vyovyote hatakosa kuadhibu,[e] anayeleta adhabu kwa ajili ya kosa la baba juu ya wana, juu ya kizazi cha tatu na juu ya kizazi cha nne.'[f] **19** Usamehe, tafadhali, kosa la watu hawa kulingana na ukuu wa fadhili zako zenye upendo, na kama vile ambavyo umewasamehe watu hawa tangu Misri na kuendelea mpaka sasa."[g]

20 Ndipo Yehova akasema: "Ninasamehe kulingana na neno lako.[h] **21** Na, kwa upande mwingine, kama ninavyoishi, dunia yote itajaa utukufu wa Yehova.[i] **22** Lakini watu wote ambao wamekuwa wakiuona utukufu[j] wangu na ishara[k] zangu ambazo nimefanya katika Misri na nyikani na bado wakaendelea kunijaribu[l] mara kumi hizi, nao hawakuisikiliza sauti yangu,[m] **23** hawataiona kamwe nchi ambayo niliwaapia baba zao, naam, wale wote wanaonitendea bila heshima hawataiona.[n] **24** Naye mtumishi wangu Kalebu,[o] kwa sababu roho iliyo tofauti ilionekana kuwa pamoja naye, naye aliendelea kunifuata kikamilifu,[p] nitamwingiza katika nchi ambamo ameenda, na wazao wake wataimiliki.[q] **25** Huku Waamaleki na Wakanaani[r] wakiwa wanakaa katika nchi tambarare ya chini, geukeni kesho na kuondoka ili mpige mwendo kuelekea nyikani kupitia njia ya Bahari Nyekundu."[s]

SURA 14

a Kut 3:8
b Kum 9:7
c Kum 7:18
Kum 20:3
d Hes 24:8
e Mwa 48:21
Kut 33:16
Kum 20:1
Isa 41:10
Ro 8:31
f Zb 27:14
g Kut 17:4
h Kut 16:10
Kut 24:17
i Hes 14:23
j Kut 16:28
k Kum 9:23
Zb 78:42
Zb 106:24
Yoh 12:37
Ebr 3:19
l Kut 32:10
m Kut 32:12
Eze 20:9
n Kut 15:14
Yos 2:10
Yos 5:1
o Kum 4:12
Kum 5:4
p Kut 13:21
Ne 9:12
Zb 78:14
Zb 105:39
q Amu 6:16
r Kum 9:28
Kum 32:27
Yos 7:9

Safu ya 2

a Zb 62:11
Zb 147:5
b Kut 34:6
Ro 9:22
c Zb 103:8
Yon 4:2
Mik 7:18
d Kut 34:7
1Yo 1:9
e Nah 1:3
Ro 2:5
f Kut 34:7
g Kut 34:9
Zb 78:38
h Yak 5:16
i Zb 72:19
Hab 2:14
j Kum 1:31
k Ne 9:17
l Kut 17:2
Zb 95:9
Zb 106:14
Ebr 3:16
m Zb 81:11
n Hes 26:64
Hes 32:11
Kum 1:35
Zb 95:11
Zb 106:26
Ebr 3:18
Ebr 4:3
o Hes 13:30
Hes 26:65
p Yos 14:9
q Yos 14:14
r Hes 13:29
s Kum 1:40

26 Naye Yehova akasema na
Musa na Haruni, na kumwa-
mbia: **27** "Kusanyiko hili le-
nye uovu litaendelea kuwa na
manung'uniko haya ambayo li-
naendeleza juu yangu mpa-
ka wakati gani?[a] Nimesikia ma-
nung'uniko ya wana wa Israeli
wanayonung'unika juu yangu.[b]
28 Waambie, '"Kama ninavyo-
ishi," asema Yehova, "ikiwa si-
tawafanyia ninyi vile ambavyo
mmesema masikioni mwangu![c]
29 Katika nyika hii mizoga
yenu itaanguka,[d] naam, wote
kati ya hesabu yenu ya walioa-
ndikishwa kuanzia miaka 20 na
zaidi, ninyi ambao mmenung'u-
nika juu yangu.[e] **30** Nanyi ha-
mtaingia katika nchi ambayo
niliinua mkono wangu katika
kiapo[f] ya kwamba nitakaa pa-
moja nanyi, isipokuwa Kalebu
mwana wa Yefune na Yoshua
mwana wa Nuni.[g]
31 ""Nao watoto wenu wa-
dogo mliosema watakuwa nya-
ra,[h] hao pia hakika nitawai-
ngiza, nao kwa kweli wata-
ijua nchi ambayo mmeikataa.[i]
32 Lakini mizoga yenu wenye-
we itaanguka katika nyika hii.[j]
33 Na wana wenu watakuwa
wachungaji nyikani[k] kwa mia-
ka 40, nao watajibu kwa saba-
bu ya matendo yenu ya uasha-
rati,[l] mpaka mizoga yenu itaka-
pofikia mwisho wake nyikani.[m]
34 Kwa hesabu ya siku mlizo-
ipeleleza nchi hiyo, siku 40,[n]
siku moja kwa mwaka mmoja,
siku moja kwa mwaka mmoja,[o]
mtajibu kwa sababu ya makosa
yenu miaka 40,[p] kwa maana la-
zima mjue maana ya mimi ku-
tenganishwa nanyi.[q]
35 ""Mimi Yehova nimese-
ema hakika hilo ndilo nitakalo-
litendea kusanyiko hili lote le-
nye uovu,[a] wale ambao wame-
kusanyika pamoja dhidi ya-
ngu: Katika nyika hii watafikia
mwisho wao, na humo wata-
kufa.[b] **36** Na wale wanaume
ambao Musa aliwatuma kuipe-
leleza nchi na ambao, waliporu-
di, walianza kulifanya kusanyi-
ko lote linung'unike juu yangu,
kwa kuleta habari mbaya juu
ya nchi hiyo,[c] **37** naam, wa-
naume walioleta habari mbaya
juu ya nchi watakufa kwa tau-
ni mbele za Yehova.[d] **38** Laki-
ni Yoshua mwana wa Nuni na
Kalebu mwana wa Yefune wa-
taendelea kuishi, kati ya wale
wanaume walioenda kuipeleele-
za nchi.""[e]
39 Musa alipowaambia wana
wote wa Israeli maneno hayo,
ndipo watu wakaanza kuom-
boleza sana.[f] **40** Na zaidi
ya hayo, wakaamka asubuhi
na mapema na kujaribu kwe-
nda juu ya mlima, wakisema:
"Tazama, sisi tutapanda mpa-
ka mahali ambapo Yehova alita-
ja. Kwa maana tumetenda dha-
mbi."[g] **41** Lakini Musa akasee-
ma: "Kwa nini mnavunja agi-
zo la Yehova?[h] Lakini jambo
hilo halitafanikiwa. **42** Msi-
pande, kwa sababu Yehova ha-
yuko katikati yenu, msije mka-
shindwa mbele ya adui zenu.[i]
43 Kwa maana Waamaleki na
Wakanaani wako huko mbele
yenu;[j] nanyi hakika mtaanguka
kwa upanga, kwa sababu mlige-
uka na kuacha kumfuata Yeho-
va, Yehova hataendelea kuwa
pamoja nanyi."[k]
44 Hata hivyo, wakafanya
kimbelembele kupanda mpa-
ka juu ya mlima,[l] lakini sandu-
ku la agano la Yehova na Musa
hawakuondoka katikati ya ka-
mbi.[m] **45** Ndipo Waamaleki[n]

SURA 14
a Kut 16:28
Hes 14:11
b 1Ko 10:10
c Hes 14:2
Hes 26:64
Hes 32:11
Kum 1:35
d 1Ko 10:5
Ebr 3:17
e Hes 1:45
Yud 5
f Kut 6:8
g Hes 26:65
Hes 32:12
Kum 1:36
Kum 1:38
h Hes 14:3
Kum 1:39
i Zb 106:24
j Zb 106:26
1Ko 10:5
Ebr 3:17
Yud 5
k Hes 32:13
Yos 14:10
l Eze 16:26
Yak 4:4
m Kum 1:3
Kum 2:14
n Hes 13:25
o Eze 4:6
p Zb 95:10
Mdo 7:36
Mdo 13:18
q Zb 60:1
Zb 108:11

Safu ya 2
a Hes 23:19
b Hes 14:29
Ebr 3:17
c Hes 13:32
d 1Ko 10:10
Yud 5
e Hes 14:30
Hes 26:65
Hes 32:12
Kum 1:36
Yos 14:6
f Kut 33:4
g Kum 1:41
h Law 26:14
2Fa 21:15
2Nya 24:20
i Law 26:17
Kum 1:42
Kum 28:25
j Hes 13:29
k Yos 6:13
2Nya 15:2
l Kum 1:43
Met 21:24
m Hes 10:33
n Kum 1:44

na Wakanaani waliokuwa wakikaa katika mlima huo wakashuka na kuanza kuwapiga nao wakawatawanya mpaka Horma.[a]

15 Na Yehova akazidi kusema na Musa, na kumwambia: **2** "Sema na wana wa Israeli, nawe utawaambia, 'Mwishowe mtakapoingia katika nchi ya makao yenu, ambayo nitawapa,[b] **3** nanyi mtamtolea Yehova toleo linalotolewa kwa njia ya moto,[c] toleo la kuteketezwa[d] au dhabihu ili kufanya nadhiri ya pekee au kwa hiari[e] au wakati wa sherehe zenu za majira,[f] ili kumfanyia Yehova harufu yenye kutuliza,[g] kutoka katika mifugo au kutoka katika kundi; **4** yule anayetoa toleo lake pia atamtolea Yehova toleo la nafaka la unga laini,[h] sehemu ya kumi ya efa, uliotiwa sehemu ya nne ya hini ya mafuta. **5** Nawe utatoa divai iwe toleo la kinywaji,[i] sehemu ya nne ya hini, pamoja na lile toleo la kuteketezwa au kwa ajili ya dhabihu ya kila mwanakondoo dume. **6** Au kwa ajili ya kondoo-dume utatoa toleo la nafaka la sehemu mbili za kumi za unga laini, uliotiwa sehemu ya tatu ya hini ya mafuta. **7** Nawe utatoa divai iwe toleo la kinywaji, sehemu ya tatu ya hini, kama harufu ya kumtuliza Yehova.

8 "'Lakini ikiwa utatoa dume la mifugo liwe toleo la kuteketezwa[j] au dhabihu ili kuweka nadhiri[k] ya pekee au dhabihu za ushirika kwa Yehova,[l] **9** mtu atatoa pia pamoja na yule dume wa mifugo, toleo la nafaka[m] la sehemu tatu za kumi za unga laini, uliotiwa nusu hini ya mafuta. **10** Nawe unapaswa kutoa divai iwe toleo la kinywaji,[a] nusu hini, kama toleo linalotolewa kwa njia ya moto, lenye harufu ya kumtuliza Yehova. **11** Hivyo ndivyo inavyopaswa kufanywa kwa ajili ya kila ng'ombe-dume au kwa ajili ya kila kondoo-dume au kwa ajili ya kichwa kimoja kati ya mwana-kondoo dume au kati ya mbuzi. **12** Hesabu yoyote ile mtakayotoa, hivyo ndivyo mnavyopaswa kufanya kwa ajili ya kila mmoja kulingana na hesabu yao. **13** Kila mwenyeji anapaswa kuwatoa hao kwa njia hiyo katika kutoa toleo linalotolewa kwa njia ya moto, lenye harufu ya kumtuliza Yehova.[b]

14 "'Na ikiwa mkaaji mgeni atakaa pamoja nanyi akiwa mgeni au mtu aliye katikati yenu kwa vizazi vyenu, naye atoe toleo linalotolewa kwa njia ya moto, lenye harufu ya kumtuliza Yehova, kama vile mnavyopaswa kufanya, ndivyo anavyopaswa kufanya.[c] **15** Ninyi mlio wa kutaniko na yule mkaaji mgeni anayekaa akiwa mgeni mtakuwa na sheria moja.[d] Itakuwa sheria mpaka wakati usio na kipimo kwa ajili ya vizazi vyenu. Mkaaji mgeni atakuwa sawa nanyi mbele za Yehova.[e] **16** Kutakuwa na sheria moja na uamuzi mmoja wa hukumu kwa ajili yenu na kwa ajili ya mkaaji mgeni anayekaa akiwa mgeni pamoja nanyi.'"[f]

17 Na Yehova akaendelea kumwambia Musa, na kusema: **18** "Sema na wana wa Israeli, nawe utawaambia, 'Mtakapoingia katika nchi ambamo nitawapeleka ninyi,[g] **19** itatukia kwamba mtakapokula mkate wowote wa nchi hiyo,[h]

SURA 14
a Hes 21:3

SURA 15
b Mwa 15:18
Kum 7:1
c Law 1:2
d Law 1:3
e Law 7:16
Law 22:18
Law 22:21
f Law 23:4
Hes 28:16
Hes 29:1
Kum 16:13
Kum 16:16
g Mwa 8:21
Law 1:9
Efe 5:2
h Kut 29:40
Law 2:1
Law 2:11
i Hes 28:7
Hes 28:14
2Ti 4:6
j Law 1:3
k Law 7:16
l Law 3:1
Law 3:3
Law 7:11
m Law 6:14
Law 7:37
Hes 28:12
Hes 29:6
1Nya 21:23

Safu ya 2
a Hes 28:14
b Mwa 8:21
Law 1:9
Law 3:16
Eze 20:41
c Kut 12:49
Law 22:18
Law 24:22
Hes 9:14
d Hes 15:29
e Law 19:34
Law 20:2
Law 24:16
Ro 3:29
f Law 16:29
Law 17:15
Hes 15:14
g Law 23:10
Kum 7:1
Kum 26:1
h Yos 5:11
Yos 5:12

mtamtolea Yehova mchango.
20 Mtatoa mchango wa ma-
zao ya kwanza[a] ya unga wenu
wenye chenga-chenga ukiwa
keki za mviringo. Kama uli-
vyo mchango wa uwanja wa
kupuria ndivyo mtakavyoutoa
mchango huo. **21** Sehemu ya
mazao ya kwanza ya unga wenu
wenye chenga-chenga mtaitoa
ikiwa mchango kwa Yehova ka-
tika vizazi vyenu vyote.

22 "'Sasa ikiwa mtafanya
kosa bila kukusudia nanyi
mkose kushika amri zote hizi,[b]
ambazo Yehova amemwambia
Musa, **23** yote ambayo Yeho-
va amewaamuru ninyi kupitia
Musa tangu siku ambayo Ye-
hova alitoa amri na kuende-
lea kwa ajili ya vizazi vyenu,
24 ndipo itatukia kwamba iki-
wa limefanywa mbali na ma-
cho ya kusanyiko kwa kukosea
bila kukusudia, kusanyiko lote
litatoa ng'ombe-dume mchanga
awe toleo la kuteketezwa kwa
ajili ya harufu ya kumtuliza Ye-
hova, na toleo lake la nafaka na
toleo lake la kinywaji kulinga-
na na utaratibu wa kawaida,[c]
na mwana-mbuzi mmoja awe
toleo la dhambi.[d] **25** Naye ku-
hani atafanya upatanisho[e] kwa
ajili ya kusanyiko lote la wana
wa Israeli, nao watasamehe-
wa; kwa sababu lilikuwa kosa
ambalo hawakukusudia,[f] nao
walileta mbele za Yehova toleo
linalotolewa kwa njia ya moto
kwa Yehova na toleo lao la dha-
mbi kwa ajili ya kosa lao amba-
lo hawakukusudia. **26** Nalo
kusanyiko lote la wana wa Isra-
eli na mkaaji mgeni anayekaa
akiwa mgeni katikati yao lita-
samehewa,[g] kwa sababu watu
wote hao walifanya kosa bila
kukusudia.

SURA 15
a Kut 23:19
Law 2:14
Hes 18:12
Kum 26:2
Kum 26:10
Ne 10:37
Met 3:9
b Zb 19:12
Yak 4:17
c Hes 15:8
Hes 15:10
d Law 4:23
Hes 28:15
2Nya 29:21
Ezr 6:17
Ezr 8:35
e Law 4:20
Ebr 2:17
1Yo 2:2
f Ebr 10:17
Yak 4:17
g Kut 34:9
Law 16:30

Safu ya 2
a Zb 19:12
Mdo 17:30
b Law 4:28
c Law 4:35
d Kut 12:49
Law 24:22
Hes 9:14
Hes 15:15
e Kut 21:14
Kum 1:43
Kum 17:12
Ebr 10:26
f Law 24:11
Isa 37:23
g Law 24:14
h Isa 30:12
1Th 4:8
i Law 26:15
j Hes 14:18
Ebr 10:28
k Law 5:1
Hes 27:3
Eze 18:20
l Kut 20:10
Kut 35:2
Kum 5:14
m Law 24:12
n Kut 31:14
o Law 24:14

27 "'Na ikiwa nafsi yoyo-
te itatenda dhambi bila ku-
kusudia,[a] basi itatoa mbuzi-
jike katika mwaka wake wa
kwanza awe toleo la dhambi.[b]
28 Naye kuhani atafanya upa-
tanisho kwa ajili ya nafsi hiyo
iliyofanya kosa kwa kutenda
dhambi mbele za Yehova bila
kukusudia, ili kuifanyia upa-
tanisho, naye atasamehewa.[c]
29 Kama ilivyo kwa mwenyeji
kati ya wana wa Israeli na mka-
aji mgeni anayekaa akiwa mge-
ni katikati yao, kutakuwa na
sheria moja kwenu juu ya kufa-
nya jambo bila kukusudia.[d]

30 "'Lakini nafsi inayofa-
nya jambo kwa kukusudia,[e]
awe ni mwenyeji au mkaaji
mgeni, aseme vibaya juu ya Ye-
hova,[f] katika hali hiyo nafsi
hiyo lazima ikatiliwe mbali ku-
toka katikati ya watu wake.[g]
31 Kwa sababu ni neno la Ye-
hova ambalo amedharau[h] na
ni amri yake ambayo amevu-
nja,[i] nafsi hiyo lazima itakatili-
wa mbali.[j] Kosa lake mwenyewe
liko juu yake.'"[k]

32 Wana wa Israeli walipoku-
wa nyikani, siku moja walimku-
ta mtu akikusanya kuni siku ya
sabato.[l] **33** Ndipo wale walio-
mkuta akikusanya kuni waka-
mleta kwa Musa na Haruni na
kusanyiko lote. **34** Kwa hiyo
wakamtia kifungoni,[m] kwa sa-
babu haikuwa imeelezwa wazi-
wazi afanywe nini.

35 Baada ya muda Yehova
akamwambia Musa: "Mtu huyo
lazima auawe,[n] kusanyiko lote
litampiga kwa mawe nje ya ka-
mbi."[o] **36** Basi kusanyiko lote
likamtoa nje ya kambi na ku-
mpiga kwa mawe mpaka aka-
fa, kama vile Yehova alivyoku-
wa amemwamuru Musa.

37 Naye Yehova akaendelea
kumwambia Musa: **38** "Sema
na wana wa Israeli, nawe uta-
waambia wajifanyie upindo we-
nye nyuzinyuzi kwenye mi-
isho ya nguo zao katika vi-
zazi vyao vyote, nao wataweka
uzi wa bluu juu ya upindo we-
nye nyuzinyuzi wa miisho ya
nguo,[a] **39** 'Nao utakuwa upi-
ndo wenye nyuzinyuzi kwa aji-
li yenu, nanyi mtauona na ku-
kumbuka amri[b] zote za Yeho-
va na kuzishika, wala hamtai-
fuata mioyo yenu na macho
yenu,[c] ambayo mnayafuata ka-
tika uasherati.[d] **40** Kusudi ni
kwamba mpate kukumbuka
na kushika amri zangu zote
na kuwa watakatifu kwa Mu-
ngu wenu.[e] **41** Mimi ni Yeho-
va Mungu wenu, ambaye nime-
watoa katika nchi ya Misri ili
niwe Mungu wenu.[f] Mimi ni Ye-
hova Mungu wenu.'"[g]

16 Na Kora[h] mwana wa Isha-
ri,[i] mwana wa Kohathi,[j]
mwana wa Lawi,[k] akaondoka,
pamoja na Dathani[l] na Abira-
mu[m] wana wa Eliabu,[n] na Oni
mwana wa Pelethi, wana wa
Rubeni.[o] **2** Nao wakasimama
mbele ya Musa, wao na watu 250
kati ya wana wa Israeli, wakuu
wa kusanyiko, walioitwa kutoka
kati ya mkutano, wanaume we-
nye sifa. **3** Basi wakakutana
dhidi ya[p] Musa na Haruni na ku-
waambia: "Imetosha, kwa sa-
babu kusanyiko lote, wote hao ni
watakatifu[q] na Yehova yuko kati-
kati yao.[r] Kwa nini, basi, mjiinue
wenyewe juu ya kutaniko la Ye-
hova?"[s]
4 Musa aliposikia jambo hilo
mara moja akaanguka kifu-
difudi. **5** Ndipo akasema na
Kora na kusanyiko lake lote, na
kuwaambia: "Asubuhi Yehova
atajulisha ni nani aliye wake[a]
na ni nani aliye mtakatifu[b]
na ni nani anayeweza kumka-
ribia,[c] na yeyote atakayemcha-
gua[d] huyo atamkaribia. **6** Fa-
nyeni hivi: Chukueni vyete-
zo[e] kwa ajili yenu, Kora na ku-
sanyiko[f] lake lote, **7** na mtie
moto ndani yake na kutia uvu-
mba juu yake mbele za Yehova
kesho, na itatukia kwamba mtu
ambaye Yehova atamchagua,[g]
yeye ndiye mtakatifu. Imeto-
sha, enyi wana wa Lawi!"[h]
8 Na Musa akaendelea ku-
mwambia Kora: "Sikilizeni, ta-
fadhali, enyi wana wa Lawi.
9 Je, ni jambo dogo sana kwe-
nu ya kwamba Mungu wa Isra-
eli amewatenga[i] ninyi mbali na
kusanyiko la Israeli ili kuwale-
ta ninyi kwake mpate kuende-
leza utumishi wa maskani ya
Yehova na kusimama mbele ya
kusanyiko ili kuwahudumia,[j]
10 na kwamba amewaleta ka-
ribu ninyi na ndugu zenu wote
wana wa Lawi? Basi, je, ni la-
zima pia ninyi mjaribu kunya-
kua ukuhani?[k] **11** Kwa saba-
bu hiyo wewe na kusanyiko
lako lote wanaokusanyika pa-
moja mnampinga Yehova.[l] Na
Haruni, yeye ni nani hata mnu-
ng'unike juu yake?"[m]
12 Baadaye Musa akatuma
watu wawaite Dathani na Abi-
ramu[n] wana wa Eliabu, lakini
wakasema: "Sisi hatutakuja![o]
13 Je, ni jambo dogo sana kwa-
mba umetuleta kutoka katika
nchi inayotiririka maziwa na
asali ili kutuua nyikani,[p] hivi
kwamba ujaribu pia kujifa-
nya mkuu juu yetu kabisa?[q]
14 Kama ilivyo, hujatuleta ka-
tika nchi inayotiririka mazi-
wa na asali,[r] upate kutupa uri-
thi wa shamba na shamba la

SURA 15
a Kum 22:12; Mt 23:5; Lu 8:44
b Kum 11:18
c Kum 29:19; Amu 17:6; Ayu 31:7; Yer 9:14
d Kut 34:15; Zb 106:39; Yak 4:4
e Law 11:44; Ro 12:1; 1Pe 1:15
f Mwa 17:8; Kut 29:45; Law 25:38
g Kut 3:15; Kut 6:2; Law 22:33

SURA 16
h Hes 26:9; Hes 27:3; Yud 11
i Kut 6:21; Hes 3:19
j Kut 6:18
k Kut 6:16; Hes 3:17
l Hes 26:9
m Kum 11:6
n Hes 26:8
o Mwa 46:8; 1Nya 5:1
p Hes 12:1; Hes 14:2; 1Sa 15:23; Zb 106:16
q Kut 19:6
r Kut 29:45; Hes 14:14
s Hes 12:2

Safu ya 2
a 2Ti 2:19
b Law 21:6
c Kut 28:43; Law 10:3
d Kut 28:1; Hes 17:5; 1Sa 2:28; Zb 105:26
e Law 10:1; Hes 16:38
f Hes 16:2
g Hes 3:10
h Hes 16:1
i Hes 3:9; Hes 3:41
j Hes 1:53; Hes 3:6; Hes 4:4; Kum 10:8
k Met 13:10; Flp 2:3
l Lu 10:16
m Kut 16:8; Zb 106:16
n Hes 16:1
o 1Sa 15:23; Yud 8
p Kut 16:3; Hes 14:29
q Kut 22:28; Mdo 7:35
r Kut 3:8; Law 20:24

mizabibu. Je, macho ya watu
hawa ndiyo unayotaka kuto-
boa? Sisi hatutakuja!"
15 Basi Musa akakasirika
sana na kumwambia Yehova:
"Usigeuke ili kutazama toleo
lao la nafaka.[a] Hata punda-
dume mmoja sijachukua ku-
toka kwao, wala sijamuumiza
mmoja wao."[b]
16 Ndipo Musa akamwa-
mbia Kora:[c] "Wewe na kusanyi-
ko lako lote, muwepo mbele za
Yehova[d] kesho, wewe na wao
na Haruni. **17** Na kila mmoja
achukue chetezo chake, nanyi
mtie uvumba juu yake na ku-
leta kila mmoja chetezo chake
mbele za Yehova, vyetezo 250,
na wewe na Haruni kila mmoja
chetezo chake." **18** Basi wa-
kachukua kila mmoja chetezo
chake, wakatia moto juu yake,
wakatia uvumba juu yake, wa-
kasimama kwenye mwingilio
wa hema la mkutano pamoja
na Musa na Haruni. **19** Kora
alipokuwa amekusanya kusa-
nyiko[e] lote pamoja dhidi yao
kwenye mwingilio wa hema
la mkutano, ndipo utukufu wa
Yehova ukalitokea kusanyiko[f]
lote.
20 Sasa Yehova akasema na
Musa na Haruni, na kuwaa-
mbia: **21** "Jitengeni[g] wenye-
we kutoka katikati ya kusa-
nyiko hili, nipate kuwaangami-
za[h] wao mara moja." **22** Ndi-
po wakaanguka kifudifudi na
kusema: "Ee Mungu, Mungu wa
roho za kila namna ya mwili,[i]
je, mtu mmoja tu atatenda dha-
mbi nawe ulikasirikie kusanyi-
ko lote?"[j]
23 Basi Yehova akasema
na Musa, na kumwambia:
24 "Sema na kusanyiko, na ku-
waambia, 'Ondokeni kuzungu-
ka pande zote za maskani za
Kora, Dathani na Abiramu!'"[a]
25 Kisha Musa akaondoka
na kwenda kwa Dathani na
Abiramu, na wanaume wa-
zee[b] wa Israeli wakaenda pamo-
ja naye. **26** Ndipo akasema
na kusanyiko, na kuwaambia:
"Geukeni kando, tafadhali, ku-
toka mbele ya mahema ya watu
hawa waovu wala msiguse cho-
chote kilicho chao,[c] msije
mkafagiliwa mbali katika dha-
mbi yao yote." **27** Wakaondo-
ka mara moja kutoka mbele ya
maskani ya Kora, Dathani na
Abiramu, kutoka pande zote,
nao Dathani na Abiramu waka-
toka nje, wakasimama kwenye
mwingilio wa mahema yao,[d] pa-
moja na wake zao, na wana wao
na watoto wao wadogo.
28 Ndipo Musa akasema:
"Kwa jambo hili mtajua kwa-
mba Yehova amenituma nifa-
nye matendo yote haya,[e] kwa-
mba si kutoka moyoni mwangu
mwenyewe:[f] **29** Ikiwa watu
hawa watakufa kifo cha wana-
damu wote na kwamba adha-
bu iletwe juu yao kulingana
na adhabu ya wanadamu
wote,[g] basi si Yehova aliyenitu-
ma mimi.[h] **30** Lakini ikiwa ni
kitu fulani kilichoumbwa amba-
cho Yehova ataumba,[i] nayo nchi
ifungue kinywa chake na ku-
wameza[j] na kila kitu kilicho
chao, nao washuke chini waki-
wa hai mpaka katika Kaburi,*[k]
ndipo hakika mtajua kwamba
watu hawa wamemtendea Yeho-
va bila heshima."[l]
31 Na ikawa kwamba mara
tu alipomaliza kusema mane-
no hayo, nchi iliyokuwa chini
yao ikaanza kupasuka na ku-
tengana.[m] **32** Nayo dunia ika-

SURA 16
a Mwa 4:5
b 1Sa 12:3
Mdo 20:33
2Ko 7:2
1Pe 3:16
c Hes 16:6
d 1Sa 12:7
e Hes 16:2
Hes 16:40
f Hes 12:5
Hes 14:10
g Mwa 19:15
Ufu 18:4
h Hes 3:10
Hes 3:38
Hes 16:45
Zb 73:19
i Hes 27:16
Ayu 12:10
Mhu 3:19
Mhu 12:7
Zek 12:1
j Mwa 18:23
2Sa 24:17

Safu ya 2
a Hes 16:1
b Hes 11:16
c Kut 23:2
d Ayu 9:4
Met 16:18
Met 18:12
e Kut 3:12
Kum 18:22
Yoh 5:36
f Kut 7:2
Kut 25:22
Kum 18:18
Yoh 5:30
g Mhu 3:19
Mhu 9:5
Eze 18:4
Ro 5:12
h Kum 18:21
i Isa 45:7
j Ayu 31:3
k Zb 55:15
Met 1:12
l Zb 74:18
Zb 107:11
m Hes 26:10
Kum 11:6
Zb 106:17

Hes 16:30* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

fungua kinywa chake na kuwameza wao na nyumba zao na wanadamu wote waliokuwa wa Kora na mali zote.[a] **33** Kwa hiyo wakashuka chini, na wote waliokuwa wao, wakiwa hai mpaka katika Kaburi,* nayo dunia ikawafunika,[b] hivi kwamba wakaangamia kutoka katikati ya kutaniko.[c] **34** Na Waisraeli wote waliokuwa wamewazunguka wakakimbia kwa sababu ya kilio chao, kwa maana walianza kusema: "Tunaogopa kwamba huenda dunia ikatumeza sisi!"[d] **35** Na moto ukaja kutoka kwa Yehova[e] na kuwateketeza wale wanaume 250 waliokuwa wakitoa uvumba.[f]

36 Sasa Yehova akasema na Musa, na kumwambia: **37** "Mwambie Eleazari mwana wa Haruni kuhani kwamba achukue vyetezo[g] hivyo kutoka katika moto, 'Nawe utawanye moto pale; kwa maana ni vitakatifu, **38** naam, vyetezo vya wanaume hao waliozitendea dhambi nafsi zao wenyewe.[h] Nao watavifanya viwe mabamba membamba ya madini ya kutanda madhabahu,[i] kwa sababu walivitoa mbele za Yehova, hivi kwamba vikawa vitakatifu; navyo vitakuwa ishara kwa wana wa Israeli.'"[j] **39** Basi Eleazari kuhani akachukua vile vyetezo vya shaba,[k] ambavyo wale waliokuwa wameteketezwa walikuwa wametoa, nao wakavifua vikawa vya kutanda madhabahu, **40** kuwa ukumbusho kwa wana wa Israeli, kusudi mgeni[l] yeyote ambaye si uzao wa Haruni asikaribie ili kufukiza uvumba mbele za Yehova,[a] wala yeyote asiwe kama Kora na kusanyiko lake,[b] kama vile Yehova alivyokuwa amesema naye kupitia Musa.

41 Na kesho yake kusanyiko lote la wana wa Israeli likaanza kunung'unika juu ya Musa na Haruni,[c] na kusema: "Ninyi, ninyi mmewaua watu wa Yehova." **42** Na ikawa kwamba kusanyiko lilipokuwa limekutanika dhidi ya Musa na Haruni, ndipo walipogeuka kulielekea hema la mkutano; na, tazama! wingu likalifunika, nao utukufu wa Yehova ukaanza kutokea.[d]

43 Naye Musa na Haruni wakaja mbele ya hema la mkutano.[e] **44** Ndipo Yehova akasema na Musa, na kumwambia: **45** "Ondokeni kutoka katikati ya kusanyiko hili, nipate kuliangamiza mara moja."[f] Ndipo wakaanguka kifudifudi.[g] **46** Kisha Musa akamwambia Haruni: "Chukua chetezo utie ndani yake moto kutoka juu ya madhabahu[h] na kutia uvumba nawe uende kwenye kusanyiko haraka na kufanya upatanisho kwa ajili yao,[i] kwa sababu hasira imetoka usoni pa Yehova.[j] Pigo limeanza!" **47** Haruni akakichukua mara moja, kama vile Musa alivyokuwa amesema, naye akakimbia kuingia katikati ya kutaniko; na, tazama! pigo lilikuwa limeanza katikati ya watu. Basi akatia uvumba juu yake na kuanza kufanya upatanisho kwa ajili ya watu. **48** Naye akaendelea kusimama katikati ya wafu na walio hai.[k] Mwishowe tauni hiyo ikakomeshwa.[l] **49** Nao waliokufa kutokana na tauni hiyo wakajumlika kuwa

SURA 16
a Hes 26:11
1Nya 6:31
1Nya 6:37
b Zb 55:23
c Yud 11
d Hes 17:13
e Law 10:2
Hes 11:1
f Hes 16:17
Hes 26:10
Zb 106:18
g Hes 16:6
h 1Fa 2:23
Met 8:36
i Kut 38:1
j Hes 16:5
Hes 17:10
Hes 26:10
1Ti 5:20
k Hes 16:6
l Hes 3:10
Hes 18:7
2Nya 26:18

Safu ya 2
a 2Nya 26:16
b Zb 106:17
Yud 11
c Hes 14:2
Zb 106:13
2Pe 2:10
d Kut 16:7
Hes 14:10
Hes 16:19
e Hes 20:6
f Kut 23:21
Hes 16:21
1Ko 10:10
g Hes 16:22
h Law 6:12
i Kut 34:9
Hes 8:19
j Law 10:6
Hes 1:53
Hes 18:5
1Nya 27:24
k 2Sa 24:16
l Kut 23:21
Hes 25:8

Hes 16:33* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

elfu kumi na nne na mia saba,
mbali na wale waliokufa kwa
sababu ya Kora. **50** Mwishowe Haruni aliporudi kwa Musa
kwenye mwingilio wa hema la
mkutano, tauni hiyo ilikuwa
imekomeshwa.

17 Sasa Yehova akasema na
Musa, na kumwambia:
2 "Sema na wana wa Israe-
li nawe uchukue kutoka kwao
fimbo[a] moja kwa ajili ya kila
nyumba ya ukoo wa upande wa
baba kutoka kwa wakuu[b] wao
wote, kulingana na nyumba ya
baba yao, fimbo kumi na mbi-
li. Utaandika jina la kila mmo-
ja katika fimbo yake. **3** Na
jina la Haruni utaliandika ka-
tika fimbo ya Lawi, kwa sa-
babu kuna fimbo moja kwa aji-
li ya kichwa cha nyumba ya
baba zao. **4** Nawe utaziweka
katika hema la mkutano
mbele ya Ushuhuda[c] huo, ma-
hali ambapo mimi huwatokea
ninyi kwa ukawaida.[d] **5** Na
itatukia kwamba mtu nitakaye-
mchagua,[e] fimbo yake itachipu-
ka, nami nitakomesha manu-
ng'uniko[f] ya wana wa Israeli juu
yangu, ambayo wananung'uni-
ka juu yenu."[g]

6 Basi Musa akasema na
wana wa Israeli, na wakuu wao
wote wakampa fimbo kwa ajili
ya kila mkuu, fimbo moja kwa
kila mkuu, kulingana na nyu-
mba ya baba zao, fimbo kumi
na mbili;[h] nayo fimbo ya Haru-
ni ilikuwa kati ya fimbo zao.[i]
7 Ndipo Musa akaziweka fimbo
hizo mbele za Yehova katika
hema la Ushuhuda.[j]

8 Na ikawa kwamba kesho
yake wakati ambapo Musa alii-
ngia ndani ya hema la Ushu-
huda, tazama! fimbo ya Ha-
runi kwa ajili ya nyumba ya

SURA 17
a Kut 4:2
b Hes 1:4
Hes 1:16
c Kut 34:29
d Kut 25:22
Kut 29:42
Kut 30:36
Law 16:2
e Hes 16:5
Lu 9:35
f Hes 11:1
Hes 14:27
Hes 16:11
Hes 16:41
1Ko 10:10
g Hes 14:2
Hes 16:13
h Hes 17:2
i Hes 17:3
j Kut 38:21
Hes 17:4
Hes 18:2

Safu ya 2
a Ebr 9:4
b Hes 16:38
c Hes 20:10
Kum 9:7
Kum 31:27
Isa 1:2
d Zb 90:7
e Hes 1:51
Hes 18:4
f Hes 18:7
g Hes 16:26
Hes 16:41
Hes 16:49

SURA 18
h Kut 25:8
Law 21:12
i Kut 28:38
Law 22:9
Hes 18:23
Ebr 5:2
j Hes 3:6
Hes 8:22
Hes 16:9
k Hes 1:53
l Hes 3:25
Hes 3:31
Hes 3:36

Lawi ilikuwa imechipuka, nayo
ilikuwa ikitokeza matumba na
maua yanayochanua nayo iliku-
wa na lozi zilizoiva. **9** Ndipo
Musa akatoa nje fimbo zote ku-
toka mbele za Yehova na kuzi-
weka mbele ya wana wote wa
Israeli, nao wakatazama na ku-
chukua kila mtu fimbo yake
mwenyewe.

10 Basi Yehova akamwa-
mbia Musa: "Irudishe fimbo[a] ya
Haruni mbele ya Ushuhuda huo
iwe kitu cha kuwekwa kama
ishara[b] kwa wana wa uasi,[c]
ili manung'uniko yao yako-
me juu yangu, wasije wakafa."
11 Musa akafanya mara moja
kama vile Yehova alivyokuwa
amemwamuru. Alifanya vivyo
hivyo.

12 Nao wana wa Israeli wa-
kaanza kumwambia Musa hivi:
"Sasa bila shaka tutakata pu-
mzi, bila shaka tutaangamia,
sisi sote tutaangamia bila sha-
ka.[d] **13** Mtu yeyote anayeka-
ribia,[e] anayekuja karibu na ma-
skani ya Yehova, atakufa![f] Je, ni
lazima tukate pumzi kwa njia
hii?"[g]

18 Na Yehova akamwambia
Haruni: "Wewe na wana
wako na nyumba ya baba yako
pamoja nawe mtajibu kwa sa-
babu ya kosa dhidi ya pataka-
tifu,[h] na wewe na wana wako
pamoja nawe mtajibu kwa sa-
babu ya kosa dhidi ya ukuha-
ni wenu.[i] **2** Na uwalete kari-
bu, pia, ndugu zako wa kabi-
la la Lawi, ukoo wa baba yako,
pamoja nawe, wapate kuunga-
na nawe na wapate kukuhudu-
mia wewe,[j] wewe na wana wako
pamoja nawe, mbele ya hema
la Ushuhuda.[k] **3** Nao watashi-
ka wajibu wao kwako na waji-
bu wao kwa hema lote.[l] Ila

wasikaribie vyombo vya mahali patakatifu na madhabahu wasije wakafa,[a] wao wala ninyi. **4** Nao wataungana nawe na watashika wajibu wao kwa hema la mkutano kuhusu utumishi wote wa hema, wala mgeni yeyote asiwakaribie ninyi.[b] **5** Nanyi mtashika wajibu wenu kwa mahali patakatifu[c] na wajibu wenu kwa madhabahu,[d] ili hasira[e] zaidi isitokee juu ya wana wa Israeli. **6** Na mimi, tazama! mimi nimewachukua ndugu zenu, Walawi, kutoka katikati ya wana wa Israeli,[f] wawe zawadi kwenu,[g] kama wale waliokabidhiwa kwa Yehova ili kuendeleza utumishi wa hema la mkutano.[h] **7** Na wewe na wana wako pamoja nawe mnapaswa kuulinda ukuhani wenu juu ya kila shughuli ya madhabahu na juu ya kile kilicho ndani ya pazia;[i] nanyi mtatoa utumishi.[j] Nitawapa ukuhani wenu kama utumishi wa zawadi, na mgeni atakayesogea karibu lazima auawe."[k]

8 Na Yehova akazidi kumwambia Haruni: "Mimi nami, tazama! nimekupa wewe utunzaji wa michango inayotolewa kwa ajili yangu.[l] Vitu vyote vitakatifu vya wana wa Israeli nimekupa wewe na wana wako viwe fungu, viwe posho mpaka wakati usio na kipimo.[m] **9** Hilo litakuwa lenu kutoka katika vitu vitakatifu zaidi, kutoka katika toleo linalotolewa kwa njia ya moto, kila toleo lao pamoja na kila toleo lao la nafaka[n] na kila toleo lao la dhambi[o] na kila toleo lao la hatia,[p] ambalo watanirudishia. Ni kitu kitakatifu zaidi kwa ajili yako na wana wako. **10** Utakula katika mahali patakatifu zaidi.[q] Kila mwanamume atakula.[a] Kitakuwa kitu kitakatifu kwako.[b] **11** Na hiki ni chako: mchango[c] wa zawadi yao pamoja na matoleo yote ya kutikisa[d] ya wana wa Israeli. Nimekupa wewe na wana wako na binti zako pamoja nawe vitu hivyo,[e] viwe posho mpaka wakati usio na kipimo. Kila mtu aliye safi katika nyumba yako anaweza kula.[f]

12 "Vyote vilivyo bora katika mafuta na vyote vilivyo bora katika divai mpya na nafaka, matunda yao ya kwanza,[g] ambayo watampa Yehova, nimekupa wewe.[h] **13** Matunda yaliyoiva ya kwanza katika vyote vilivyo katika nchi yao, ambayo watamletea Yehova, yatakuwa yako.[i] Kila mtu aliye safi katika nyumba yako anaweza kula.

14 "Kila kitu kilichotolewa katika Israeli kinapaswa kuwa chako.[j]

15 "Kila kitu kinachofungua tumbo la uzazi,[k] cha kila namna yenye mwili, ambacho watamtolea Yehova, kati ya wanadamu na kati ya wanyama, kinapaswa kuwa chako. Hata hivyo, unapaswa kumkomboa mzaliwa wa kwanza wa wanadamu;[l] na mzaliwa wa kwanza wa mnyama ambaye si safi unapaswa kumkomboa.[m] **16** Na kwa bei ya ukombozi kwa ajili yake kuanzia umri wa mwezi mmoja na kuendelea utamkomboa, kwa thamani iliyokadiriwa, shekeli 5 za fedha kulingana na shekeli ya mahali patakatifu.[n] Ni gera 20.[o] **17** Ila tu ng'ombe-dume aliye mzaliwa wa kwanza au mwanakondoo dume aliye mzaliwa wa kwanza au mbuzi aliye mzaliwa wa kwanza hutawakomboa.[p] Hao ni kitu kitakatifu. Damu[q]

SURA 18

a Hes 4:15
Hes 4:20
Hes 16:40
b Hes 1:51
Hes 3:10
c Kut 27:21
Kut 30:7
Law 24:3
Hes 3:32
d Law 1:17
Law 21:17
e Hes 16:46
f Hes 3:12
Hes 3:45
g Hes 3:9
Hes 8:16
h Hes 8:19
i Law 16:2
Law 16:12
Ebr 9:3
Ebr 9:7
j 1Sa 2:28
Ebr 5:4
k Hes 3:10
Hes 16:40
l Kut 23:19
Law 27:28
Law 27:30
Hes 18:11
Hes 18:26
m Law 7:34
Hes 5:9
n Law 2:3
Law 6:16
Law 10:12
o Law 5:12
Law 6:26
Law 6:29
p Law 5:6
Law 7:1
Law 7:7
q Kut 29:32
Law 6:16
Law 10:13

Safu ya 2

a Law 6:18
Law 7:6
b Law 14:13
Law 21:22
c Kut 29:27
Hes 15:20
Eze 44:30
d Kut 29:27
Law 7:34
e Law 10:14
Kum 18:3
f Law 22:6
g Met 3:9
h Law 2:14
Kum 18:4
Ne 10:35
i Kut 23:19
j Law 27:21
Law 27:28
k Kut 13:2
Law 27:26
Hes 3:13
Lu 2:23
l Kut 13:13
m Kut 34:20
Law 27:27
n Law 27:2
Law 27:6
o Kut 30:13
Law 27:25
p Kut 22:30
Kum 15:19
q Law 17:11

yao unapaswa kuinyunyiza juu
ya madhabahu, na mafuta yao
utayafukiza kama toleo linalo-
tolewa kwa njia ya moto ili
kuwa harufu ya kumtuliza Ye-
hova.[a] **18** Na nyama yao ita-
kuwa yako. Kama vile kidari
cha toleo la kutikisa na kama
ule mguu wa kuume, inapa-
swa kuwa yako.[b] **19** Micha-
ngo yote mitakatifu,[c] ambayo
wana wa Israeli watamchangia
Yehova, nimekupa wewe na
wana wako na binti zako pamo-
ja nawe, iwe posho lenu mpa-
ka wakati usio na kipimo.[d] Ni
agano la chumvi mpaka wakati
usio na kipimo mbele za Yeho-
va kwa ajili yako na kwa ajili ya
uzao wako pamoja nawe."[e]
20 Na Yehova akaendelea
kumwambia Haruni: "Katika
nchi yao hutakuwa na urithi,
wala hakuna fungu lolote li-
takalokuwa lako katikati yao.[f]
Mimi ni fungu lako na urithi
wako katikati ya wana wa Isra-
eli.[g]
21 "Na kwa wana wa Lawi,
tazama! nimewapa kila sehemu
ya kumi[h] katika Israeli iwe uri-
thi wao kwa sababu ya utumi-
shi wao wanaofanya, utumishi
wa hema la mkutano. **22** Na
wana wa Israeli wasikaribie
tena hema la mkutano wasije
wakawa na hatia ya dhambi na
kufa.[i] **23** Nao Walawi wenye-
we wataendeleza utumishi wa
hema la mkutano, nao ndio wa-
naopaswa kujibu kwa kosa lao.[j]
Ni sheria mpaka wakati usio na
kipimo katika vizazi vyenu vyo-
te kwamba katikati ya wana wa
Israeli hawapaswi kupata uri-
thi.[k] **24** Kwa maana ile sehe-
mu ya kumi ya wana wa Israeli,
ambayo watamchangia Yehova
kuwa mchango, nimewapa Wa-

SURA 18
a Law 3:16
b Kut 29:26
Law 7:31
Law 7:34
c Kut 23:19
Hes 15:19
Hes 18:11
Hes 18:26
Hes 31:29
d Hes 18:8
2Nya 31:4
e Law 2:13
2Nya 13:5
f Hes 26:62
Kum 10:9
Kum 12:12
Kum 14:27
Yos 14:3
g Kum 18:2
Yos 13:14
Yos 18:7
Eze 44:28
h Law 27:30
2Nya 31:5
Ne 10:37
Ne 12:44
Ne 13:12
Ga 6:6
Ebr 7:5
i Hes 16:40
Hes 17:13
j Hes 3:7
Hes 18:1
k Yos 13:33

Safu ya 2
a Kum 10:9
b Hes 18:21
Kum 12:19
c Ne 10:38
Ebr 7:9
d Hes 15:20
e Hes 18:12
f Met 3:9
g Mt 10:10
Lu 10:7
1Ko 9:9
1Ko 9:13
Ga 6:6
1Ti 5:18

lawi kuwa urithi. Ndiyo saba-
bu nimewaambia, 'Katikati ya
wana wa Israeli hawapaswi ku-
pata urithi.'"[a]
25 Ndipo Yehova akasema
na Musa, na kumwambia:
26 "Na wewe utasema na Walawi,
nawe utawaambia, 'Mtapo-
kea kutoka kwa wana wa Israe-
li sehemu ya kumi ambayo ni-
mewapa ninyi kutoka kwao
kwa ajili ya urithi wenu,[b] na-
nyi mtatoa mchango wenu ku-
toka katika hiyo uwe mchan-
go kwa Yehova wa sehemu ya
kumi ya hiyo sehemu ya kumi.[c]
27 Na utahesabiwa kwenu
kuwa mchango wenu, kama ile
nafaka ya uwanja wa kupuria[d]
na kama yale mazao ka-
mili ya shinikizo la divai au
la mafuta. **28** Na kwa njia
hiyo ninyi wenyewe mtachanga
mchango wenu kwa Yehova ku-
toka katika sehemu zenu zote
za kumi ambazo mtapokea ku-
toka kwa wana wa Israeli, na
katika hizo mtamtolea Yehova
mchango kwa Haruni kuhani.
29 Katika zawadi zote mtaka-
zopewa, mtachanga kila namna
ya mchango kwa Yehova, ule
ulio bora zaidi,[e] uwe kitu kita-
katifu kutoka kwao.'
30 "Nawe utawaambia, 'Mna-
pochanga vilivyo bora kuto-
ka kwa hivyo,[f] ndipo itahesa-
biwa kwa Walawi kama mazao
ya uwanja wa kupuria na kama
mazao ya shinikizo la divai au
la mafuta. **31** Nanyi mtaku-
la vitu hivyo kila mahali, ni-
nyi na nyumba yenu, kwa saba-
bu ni malipo yenu kwa ajili ya
utumishi wenu katika hema la
mkutano.[g] **32** Nanyi msijile-
tee hatia ya dhambi mnapocha-
nga vilivyo bora katika hivyo,
wala msitie unajisi vitu vitaka-

tifu vya wana wa Israeli, msije
mkafa.'"[a]

19 Na Yehova akasema na
Musa na Haruni, na ku-
waambia: **2** "Hii ni amri ya
sheria ambayo Yehova amea-
muru, na kusema, 'Waambie
wana wa Israeli kwamba waku-
chukulie ng'ombe mwekundu
aliye timamu[b] ambaye hana ka-
soro yoyote na ambaye haja-
fungwa nira yoyote.[c] **3** Nanyi
mtamkabidhi Eleazari kuha-
ni, naye atampeleka nje ya ka-
mbi, naye atachinjwa mbele
yake. **4** Kisha Eleazari kuha-
ni atachukua sehemu ya damu
yake kwa kidole chake na kui-
tapanya sehemu ya damu yake
moja kwa moja kuelekea hema
la mkutano mara saba.[d] **5** Na
ng'ombe huyo atateketezwa
motoni mbele ya macho yake.
Ngozi yake na nyama yake na
damu yake pamoja na mavi
yake vitateketezwa.[e] **6** Naye
kuhani atachukua mti wa mwe-
rezi[f] na hisopo[g] na kitambaa
chenye rangi nyekundu ya ko-
chinili[h] na kuvitupa katikati ya
moto unaomteketeza ng'ombe.
7 Naye kuhani atayafua mava-
zi yake na kuoga mwili wake
katika maji, na baadaye anawe-
za kuingia kambini; lakini yule
kuhani atakuwa si safi mpaka
jioni.

8 "'Na yule aliyemteketeza
atayafua mavazi yake katika
maji na kuoga mwili wake ka-
tika maji,[i] naye atakuwa asiye
safi mpaka jioni.

9 "'Na mwanamume aliye
safi atayakusanya majivu[j] ya
ng'ombe huyo na kuyaweka nje
ya kambi katika mahali safi;
nayo yatatumika kama kitu cha
kuwekwa kwa ajili ya yale maji
ya kutakasa kwa wana wa Isra-
eli.[a] Ni toleo la dhambi. **10** Na
yule anayekusanya majivu ya
yule ng'ombe atayafua mavazi
yake na kuwa asiye safi mpa-
ka jioni.[b]

"'Nayo itakuwa sheria mpa-
ka wakati usio na kipimo kwa
wana wa Israeli na mkaaji mge-
ni anayekaa akiwa mgeni kati-
kati yao.[c] **11** Yeyote ataka-
yegusa maiti ya nafsi[d] yoyo-
te ya binadamu atakuwa asiye
safi siku saba.[e] **12** Mtu huyo
anapaswa kujitakasa kwa maji
hayo siku ya tatu,[f] na siku ya
saba atakuwa safi. Lakini ikiwa
hatajitakasa siku ya tatu,
basi siku ya saba hatakuwa safi.
13 Kila mtu atakayegusa mai-
ti, nafsi ya mtu yeyoteataka-
yekufa, na ambaye hatajitaka-
sa, ameitia unajisi maskani ya
Yehova,[g] nayo nafsi hiyo lazi-
ma ikatiliwe mbali kutoka kati-
ka Israeli.[h] Kwa sababu maji ya
kutakasa[i] hayakunyunyizwa
juu yake, anaendelea kuwa asi-
ye safi. Uchafu wake bado uko
juu yake.[j]

14 "'Hii ndiyo sheria ikiwa
mtu atakufa ndani ya hema:
Kila mtu atakayeingia kati-
ka hema hilo, na kila mtu ali-
ye ndani ya hema hilo,ataku-
wa asiye safi siku saba. **15** Na
kila chombo[k] kilichofunguliwa
ambacho hakina kifuniko kili-
chofunikwa si safi. **16** Na kila
mtu ambaye huko shambani
atagusa mtu aliyeuawa kwa
upanga[l] au maiti au mfupa[m]
wa mtu au kaburi atakuwa
asiye safi siku saba. **17** Nao
watachukua kwa ajili ya yule
asiye safi sehemu ya mavu-
mbi ya moto wa toleo la dha-
mbi na kutia maji yanayotiriri-
ka juu ya mavumbi katika cho-
mbo. **18** Ndipo mtu aliye safi[n]

SURA 18
a Law 22:2
Law 22:15

SURA 19
b Law 22:20
Mal 1:14
1Pe 2:22
c Kum 21:3
d Ebr 9:13
1Pe 1:2
e Kut 29:14
Law 4:11
f Law 14:4
Law 14:49
g Zb 51:7
h Isa 1:18
i Law 16:28
j Ebr 9:13

Safu ya 2
a Hes 19:13
Hes 19:21
Hes 31:23
b Hes 19:8
c Kut 12:49
Law 24:22
Hes 15:15
d Law 21:1
Law 21:11
Hes 5:2
Hes 6:9
Hes 9:6
e Hes 31:19
Hag 2:13
f Hes 31:19
g Law 15:31
h Ebr 2:2
Ebr 10:28
i Hes 19:9
Hes 31:23
j Law 22:3
k Law 11:32
l Hes 31:19
m Hes 19:11
n Hes 19:9

atachukua hisopo[a] na kuichovya ndani ya maji yale na kuyatapanya juu ya hema na vyombo vyote na nafsi zote zilizokuwa hapo na juu ya yule aliyegusa mfupa au mtu aliyeuawa au maiti au kaburi. **19** Na yule mtu aliye safi atayatapanya juu ya yule asiye safi siku ya tatu na siku ya saba na kumtakasa kutokana na dhambi yake siku ya saba;[b] naye atayafua mavazi yake na kuoga katika maji, naye atakuwa safi jioni.

20 "'Lakini mtu asiye safi na ambaye hatajitakasa, basi, nafsi hiyo lazima ikatiliwe mbali[c] kutoka katikati ya kutaniko, kwa sababu amepatia unajisi patakatifu pa Yehova. Maji ya kutakasa hayakunyunyizwa juu yake. Yeye si safi.

21 "'Nayo itatumika kama sheria mpaka wakati usio na kipimo kwa ajili yao, kwamba yule anayetapanya maji kwa ajili ya kutakasa anapaswa kuyafua mavazi yake,[d] pia yule anayegusa maji ya kutakasa. Atakuwa asiye safi mpaka jioni. **22** Na kitu chochote ambacho huenda yule mtu asiye safi atakigusa kitakuwa kisicho safi,[e] nayo nafsi itakayokigusa itakuwa najisi mpaka jioni.'"[f]

20 Nao wana wa Israeli, kusanyiko lote, wakaingia katika nyika ya Zini[g] katika mwezi wa kwanza, nao watu wakakaa Kadeshi.[h] Hapo ndipo Miriamu[i] alipofia na hapo ndipo alipozikwa.

2 Sasa hapakuwa na maji kwa ajili ya kusanyiko hilo,[j] nao wakaanza kukutanika pamoja dhidi ya Musa na Haruni.[k] **3** Nao watu wakagombana[l] na Musa na kusema: "Laiti tungalikufa wakati ndugu zetu walipokufa mbele za Yehova![a] **4** Na kwa nini ninyi mmeleta kutaniko la Yehova katika nyika hii ili sisi na wanyama wetu wa kubeba mizigo tufie huko?[b] **5** Na kwa nini mmetuongoza kutoka Misri na kututuleta katika mahali hapa pabaya?[c] Si mahali pa mbegu na tini na mizabibu na makomamanga,[d] wala hapana maji ya kunywa." **6** Ndipo Musa na Haruni wakatoka mbele ya kutaniko wakaenda kwenye mwingilio wa hema la mkutano na kuanguka kifudifudi,[e] nao utukufu wa Yehova ukaanza kuwatokea.[f]

7 Ndipo Yehova akasema na Musa, na kumwambia: **8** "Ichukue fimbo[g] na kuliita kusanyiko pamoja, wewe na Haruni ndugu yako, nanyi mtauambia mwamba mbele ya macho yao ili kwa kweli utoe maji yake; nawe utawatolea maji kutoka katika mwamba na kuwapa maji kusanyiko na wanyama wao wa kubeba mizigo."[h]

9 Basi Musa akachukua fimbo kutoka mbele za Yehova,[i] kama vile alivyokuwa amemwamuru. **10** Kisha Musa na Haruni wakaliita kutaniko pamoja mbele ya mwamba, naye akawaambia: "Sikieni, sasa, enyi waasi![j] Je, tuwatolee ninyi maji katika mwamba huu?"[k] **11** Halafu Musa akainua mkono wake na kuupiga mwamba mara mbili kwa fimbo yake; na maji mengi yakaanza kutoka, nalo kusanyiko na wanyama wao wa kubeba mizigo wakaanza kunywa.[l]

12 Baadaye Yehova akawaambia Musa na Haruni: "Kwa sababu hamkuonyesha imani

SURA 19
a Zb 51:7
b Law 14:9
Hes 19:12
Hes 31:19
c Mwa 17:14
Hes 19:13
d Hes 19:18
Ebr 9:10
Ebr 9:13
e Hag 2:13
f Law 15:5

SURA 20
g Hes 13:21
Hes 33:36
h Hes 13:26
Hes 20:22
Kum 1:46
Kum 2:14
Amu 11:16
i Kut 15:20
Hes 26:59
Mik 6:4
j Kut 17:1
k Hes 16:42
l Kut 17:2

Safu ya 2
a Hes 16:35
Hes 16:41
Hes 16:49
b Kut 14:11
Kut 17:3
Hes 16:13
Hes 21:5
c Hes 16:14
Kum 8:15
Ne 9:21
d Kut 3:17
Kut 13:5
Kum 8:8
Yer 2:2
e Hes 14:5
f Kut 16:10
Hes 14:10
g Kut 17:5
h Ne 9:15
Zb 78:15
Zb 105:41
Zb 114:8
Isa 43:20
Isa 48:21
i Kut 7:12
Kut 7:19
Hes 17:10
Ebr 9:4
j Kum 9:24
Zb 106:32
k Zb 106:33
l Kut 17:6
Kum 8:15
1Ko 10:4

kwangu ili kunitakasa[a] mbele ya macho ya wana wa Israeli, kwa hiyo ninyi hamtaliingiza kutaniko hili katika nchi ambayo hakika nitawapa wao."[b]
13 Hayo ndiyo maji ya Meriba,[c] kwa sababu wana wa Israeli waligombana na Yehova, hivi kwamba akatakaswa katikati yao.

14 Basi Musa akatuma wajumbe kutoka Kadeshi mpaka kwa mfalme wa Edomu:[d] "Hivi ndivyo ndugu yako Israeli[e] amesema, 'Wewe mwenyewe unajua vema magumu yote ambayo yametupata.[f] **15** Na baba zetu walishuka Misri,[g] nasi tukaendelea kukaa Misri siku nyingi;[h] nao Wamisri wakaanza kutudhuru sisi na baba zetu.[i] **16** Mwishowe tukamlilia Yehova[j] naye akaisikia sauti yetu na kumtuma malaika,[k] akatutoa Misri; na tazama, tuko hapa Kadeshi, jiji lililo kwenye mpaka wa eneo lako. **17** Acha tupite, tafadhali, katika nchi yako. Hatutapita katika shamba wala katika shamba la mizabibu, wala hatutakunywa maji ya kisima. Katika njia ya mfalme tutapiga mwendo.[l] Hatutageuka kuelekea kuume wala kuelekea kushoto,[m] mpaka tutakapokuwa tumepita katikati ya eneo lako.'"
18 Hata hivyo, Edomu akamwambia: "Hutapita katikati yangu, nisije nikatoka nje nikiwa na upanga ili nikutane nawe." **19** Nao wana wa Israeli wakamwambia: "Kwa njia kuu tutaenda; na ikiwa mimi na mifugo yangu tutakunywa maji yako, nitalipa thamani yake.[n] Sitaki kitu chochote ila kupita kwa miguu yangu."[o] **20** Bado akasema: "Hutapita."[p] Kisha Edomu[q] akatoka nje ili kukutana naye akiwa na watu wengi sana na mkono wenye nguvu. **21** Basi Edomu akakataa kumpa Israeli ruhusa ya kupita katikati ya eneo lake.[a] Kwa hiyo Israeli akageuka na kumwacha.[b]

22 Na wana wa Israeli, kusanyiko lote, wakaondoka Kadeshi[c] nao wakafika Mlima Hori.[d] **23** Kisha Yehova akawaambia Musa na Haruni jambo hili katika Mlima Hori karibu na mpaka wa nchi ya Edomu: **24** "Haruni atakusanywa kwa watu wake,[e] kwa maana hataingia katika nchi ambayo nitawapa wana wa Israeli, kwa sababu ninyi mliasi agizo langu kuhusiana na maji ya Meriba.[f] **25** Wachukue Haruni na Eleazari mwana wake, uwalete juu kwenye Mlima Hori. **26** Nawe umvue Haruni mavazi yake,[g] nawe utamvika Eleazari[h] mwana wake mavazi hayo; naye Haruni atakusanywa, naye atakufa huko."[i]

27 Basi Musa akafanya kama vile Yehova alivyokuwa ameamuru; nao wakapanda Mlima Hori mbele ya macho ya kusanyiko lote. **28** Kisha Musa akamvua Haruni mavazi yake na kumvika Eleazari mwana wake mavazi hayo, kisha Haruni akafa huko juu ya mlima huo.[j] Naye Musa na Eleazari wakashuka kutoka mlimani. **29** Nalo kusanyiko lote likapata kuona kwamba Haruni alikuwa amekata pumzi, na nyumba yote ya Israeli ikaendelea kumlilia Haruni siku 30.[k]

21 Sasa yule Mkanaani, mfalme wa Aradi,[l] aliyekaa Negebu,[m] akapata kusikia kwamba Israeli alikuwa amekuja kupitia njia ya Atharimu, naye akaanza kupigana na

SURA 20
a Law 10:3; Hes 27:14; Kum 32:51; Isa 8:13; Ufu 4:11
b Kum 1:37; Kum 3:26; Kum 34:4; Yos 1:2
c Kum 33:8; Zb 95:8; Zb 106:32; Ebr 3:8
d Amu 11:17
e Mwa 36:8; Kum 2:4; Kum 23:7
f Kut 18:8
g Mwa 46:6; Mdo 7:15
h Mwa 15:13; Kut 12:40
i Kut 1:11; Kut 1:14; Kum 26:6; Mdo 7:19
j Kut 2:23; Kut 3:7
k Kut 14:19; Kut 23:20; Kut 33:2; Mdo 7:35
l Hes 21:22
m Kum 2:27
n Kum 2:6
o Kum 2:28
p Amu 11:17
q Mwa 36:1

Safu ya 2
a Kum 2:29
b Kum 2:8; Amu 11:18
c Hes 13:26; Hes 33:37
d Hes 21:4; Hes 34:7
e Mwa 25:8; Hes 33:38; Kum 32:50
f Hes 20:12; Kum 32:51
g Kut 28:2; Kut 29:29; Ebr 7:23
h Kut 6:23; Hes 4:16
i Hes 33:38
j Hes 33:39; Kum 10:6; Kum 32:50
k Kum 34:8

SURA 21
l Hes 33:40; Yos 12:14
m Hes 13:22

Israeli na kuchukua baadhi yao
kuwa mateka. **2** Basi Israeli
akaweka nadhiri kwa Yehova
na kusema:[a] "Hakika ukiwatia
watu hawa mkononi mwangu,
mimi pia hakika nitayaangami-
za majiji yao."[b] **3** Kwa hiyo
Yehova akaisikiliza sauti ya
Israeli na kuwakabidhi Wa-
kanaani; nao wakawaangami-
za wao na majiji yao. Kisha wa-
kapaita mahali hapo Horma.[c]

4 Walipoendelea kusafiri ku-
toka Mlima Hori[d] wakipitia njia
ya Bahari Nyekundu ili kuizu-
nguka nchi ya Edomu,[e] nafsi ya
watu ikaanza kuchoka kwa sa-
babu ya ile njia. **5** Nao watu
wakaendelea kusema dhidi ya
Mungu[f] na Musa:[g] "Kwa nini
mmetutoa Misri ili tufe nyika-
ni?[h] Kwa maana hakuna mkate
wala maji,[i] nayo nafsi yetu ime-
uchukia huu mkate wa kudha-
raulika."[j] **6** Basi Yehova aka-
tuma nyoka wenye sumu[k] kati-
kati ya watu, nao wakawa wa-
kiwauma watu, hivi kwamba
watu wengi wa Israeli wakafa.[l]

7 Mwishowe watu wakamjia
Musa na kusema: "Tumetenda
dhambi,[m] kwa sababu tumesema
dhidi ya Yehova na dhidi yako.
Tutetee kwa Yehova awaondoe
nyoka hawa juu yetu."[n] Naye
Musa akawatetea watu.[o] **8** Ndi-
po Yehova akamwambia Musa:
"Jifanyie nyoka mkali na ku-
mweka juu ya nguzo ya ishara.
Na itatukia kwamba wakati mtu
yeyote ameumwa, basi atamta-
zama na hivyo ataendelea kuwa
hai."[p] **9** Mara moja Musa akafa-
nya nyoka wa shaba[q] na kumwe-
ka juu ya nguzo ya ishara;[r] na ika-
wa kwamba nyoka alipomuuma
mtu naye akamtazama[s] yule nyo-
ka wa shaba, ndipo alipoendelea
kuwa hai.[t]

SURA 21

a Kum 23:21
b Law 27:28
Kum 20:17
Yos 6:18
c Hes 14:45
Amu 1:17
d Hes 33:41
e Hes 20:21
Kum 2:8
Amu 11:18
f Zb 78:19
g Kut 14:11
Kut 15:24
Hes 16:13
h Hes 14:28
Hes 14:34
i Hes 20:5
j Kut 16:15
Hes 11:6
Zb 78:24
k Kum 8:15
l Zb 106:43
1Ko 10:9
m Zb 78:34
n Law 26:40
o Kut 32:11
p Zb 106:44
q 2Fa 18:4
r Yoh 3:14
Yoh 8:28
Yoh 12:32
Ga 3:13
1Pe 2:24
s Yoh 1:29
Ebr 12:2
t Yoh 3:14
Yoh 3:15
Yoh 6:40
Ro 1:17

Safu ya 2

a Hes 33:43
b Hes 33:44
c Kum 2:13
d Hes 22:36
Kum 2:24
Amu 11:18
e Hes 21:28
Kum 2:18
Kum 2:29
Isa 15:1
f Isa 15:8
g Zb 78:52
h Zb 105:2
i Mwa 49:10
j Yos 13:17
k Hes 26:63
Hes 33:49
l Kum 3:27
Kum 34:1
m Hes 23:28
Yos 12:3

10 Kisha wana wa Israeli
wakaondoka na kupiga kambi
Obothi.[a] **11** Kisha wakaondo-
ka Obothi na kupiga kambi
Iye-abarimu,[b] katika nyika ina-
yoelekea upande wa mbele wa
Moabu, kuelekea mashariki.
12 Kutoka huko wakasafiri na
kupiga kambi kando ya bonde
la mto la Zeredi.[c] **13** Kutoka
huko wakasafiri na kupiga ka-
mbi katika eneo la Arnoni,[d] li-
lilo katika nyika inayosambaa
kutoka katika mpaka wa Waa-
mori; kwa maana Arnoni ni
mpaka wa Moabu, kati ya Moa-
bu na Waamori. **14** Ndiyo sa-
babu imesemwa katika kitabu
cha Vita vya Yehova:

"Vahebu katika Sufa na mabo-
nde ya mito ya Arnoni,
15 na mdomo wa mabonde ya
mito, ambao umejipinda kue-
lekea kiti cha Ari[e] na kuege-
mea juu ya mpaka wa Moabu."

16 Kisha kutoka huko hadi
Beeri.[f] Hicho ndicho kisima
ambacho Yehova alimwambia
hivi Musa juu yake: "Wakusa-
nye watu, niwape maji."[g]

17 Wakati huo Israeli waka-
anza kuimba wimbo[h] huu:

"Bubujika, Ee kisima!
Kiitikieni, enyi watu!
18 Kisima, wakuu
walikichimba. Watu
wenye vyeo kati ya watu
walikichimba,
Kwa fimbo ya kiongozi,[i]
kwa fimbo zao wenyewe."

Kisha kutoka nyikani mpa-
ka Matana. **19** Na kutoka Ma-
tana mpaka Nahalieli, na kuto-
ka Nahalieli mpaka Bamothi.[j]
20 Na kutoka Bamothi mpaka
katika bonde lililo katika uwa-
nja wa Moabu,[k] kwenye kichwa
cha Pisga,[l] nalo linachomo-
za kuelekea uso wa Yeshimoni.[m]

21 Sasa Israeli akatuma wajumbe kwa Sihoni[a] mfalme wa Waamori, na kusema: **22** "Acha nipite katikati ya nchi yako. Hatutageuka kando kuingia katika shamba wala katika shamba la mizabibu. Hatutakunywa maji ya kisima chochote. Kwenye barabara ya mfalme tutapiga mwendo mpaka tutakapokuwa tumepita katikati ya eneo lako."[b] **23** Naye Sihoni hakumruhusu Israeli apite katikati ya eneo lake,[c] bali Sihoni akawakusanya watu wake wote na kwenda kukutana na Israeli nyikani, naye akaja kule Yahazi[d] na kuanza kupigana na Israeli. **24** Ndipo Israeli akampiga kwa makali ya upanga[e] na kuitwaa nchi[f] yake kutoka Arnoni[g] hadi Yaboki,[h] karibu na wana wa Amoni; kwa sababu Yazeri[i] ndio mpaka wa wana wa Amoni.[j]

25 Basi Israeli akayachukua majiji hayo yote, naye Israeli akaanza kukaa katika majiji yote ya Waamori,[k] katika Heshboni[l] na miji yake yote ya kandokando. **26** Kwa maana Heshboni lilikuwa jiji la Sihoni.[m] Yeye alikuwa mfalme wa Waamori,[n] naye ndiye aliyepigana na mfalme wa Moabu zamani na kuichukua nchi yake yote kutoka mkononi mwake mpaka Arnoni.[o] **27** Ndiyo sababu waimbaji wa mafungu ya shairi la kufanya mzaha walisema:

"Njoo katika Heshboni.
Jiji la Sihoni na lijengwe
na kuonekana kuwa
limefanywa imara.
28 Kwa maana moto umetoka
Heshboni,[p] mwali wa
moto kutoka katika mji
wa Sihoni.
Umeteketeza Ari[a] la
Moabu, wanaomiliki
mahali pa juu pa Arnoni.
29 Ole wako, Moabu! Hakika
mtaangamia, enyi watu
wa Kemoshi![b]
Hakika atawafanya
wanawe kama watu
walioponyoka na binti
zake kuwa utekwani
mkononi mwa mfalme wa
Waamori, Sihoni.
30 Kwa hiyo na tuwapige
mishale.
Hakika Heshboni
ataangamia mpaka
Diboni,[c]
Nao wanawake mpaka
Nofa, wanaume mpaka
Medeba."[d]

31 Na Israeli akaanza kukaa katika nchi ya Waamori.[e] **32** Ndipo Musa akatuma watu fulani wakapeleleze Yazeri.[f] Kwa hiyo wakateka miji yake ya kandokando na kuwaondolea mbali Waamori waliokuwa humo.[g] **33** Baada ya hapo wakageuka, wakapanda wakipitia njia ya Bashani.[h] Ndipo Ogu[i] mfalme wa Bashani akatoka nje ili kukutana nao, yeye pamoja na watu wake wote, katika vita vya Edrei.[j] **34** Sasa Yehova akamwambia Musa: "Usimwogope,[k] kwa maana nitamtia yeye na watu wake wote na nchi yake mkononi mwako;[l] nawe utamtendea kama vile ulivyomtendea Sihoni mfalme wa Waamori, aliyekuwa akikaa Heshboni."[m] **35** Basi wakampiga yeye pamoja na wanawe na watu wake wote, mpaka ikawa hakuna mwokokaji aliyebaki kwake;[n] nao wakaitwaa nchi yake.[o]

SURA 21
a Kum 2:26; Amu 11:19
b Hes 20:17
c Kum 2:30; Kum 29:7; Amu 11:20
d Kum 2:32; Yos 13:18
e Yos 12:2; Amu 11:21; Zb 135:10; Zb 136:19; Amo 2:9
f Hes 32:33; Ne 9:22
g Hes 21:13; Kum 3:16
h Amu 11:22
i Hes 32:1; 1Nya 6:81
j Yos 12:2
k Mwa 10:16; Mwa 15:16; Kut 3:8; Kum 7:1
l Kum 2:26; Amu 11:19; Wim 7:4
m Zb 135:11
n Amu 11:19
o Hes 21:13
p Yer 48:45

Safu ya 2
a Hes 21:15; Kum 2:9
b Amu 11:24; 1Fa 11:7; 2Fa 23:13; Yer 48:7
c Hes 32:34; Yos 13:17; Yer 48:18
d Yos 13:9
e Kum 3:8
f Hes 32:1
g Hes 21:25
h Kum 3:1
i Kum 1:4; Kum 3:11; Kum 4:47; Yos 9:10
j Kum 3:10; Yos 13:12
k Kum 3:2; Kum 3:22; Kum 20:3
l Kut 23:27; Kum 7:24
m Zb 135:11
n Kum 3:3; Yos 13:12
o Yos 12:4; Yos 12:6

22 Ndipo wana wa Israeli
wakaondoka na kupiga
kambi kwenye nchi tambarare za jangwa la Moabu[a] ng'ambo ya Yordani kutoka Yeriko.
2 Na Balaki[b] mwana wa Sipori akaona mambo yote ambayo
Israeli alikuwa amewatendea
Waamori. **3** Na Moabu akawaogopa sana watu hao, kwa
sababu walikuwa wengi; na Moabu akaanza kuhofu na kuchukizwa kwa sababu ya wana wa
Israeli.[c] **4** Na Moabu akawaambia wanaume wazee wa Midiani:[d] "Sasa hili kutaniko litaramba mazingira yenu yote kama
ng'ombe anavyoramba majani
ya shambani."

Na Balaki[e] mwana wa Sipori alikuwa mfalme wa Moabu wakati huo hasa. **5** Sasa
akatuma wajumbe kwa Balaamu[f] mwana wa Beori huko Pethori,[g] kando ya Mto[h] wa nchi
ya wana wa watu wake, aitwe,
na kusema: "Tazama! Watu wametoka Misri. Tazama! Wameijaza nchi kwa kadiri ambayo
mtu anaweza kuona,[i] nao wanakaa mbele yangu. **6** Basi
sasa njoo, tafadhali; uwalaani[j] watu hawa kwa ajili yangu,
kwa maana ni wenye nguvu kuliko mimi. Huenda nitaweza kuwapiga nami niwafukuze kutoka katika nchi; kwa maana najua vema kwamba yule unayembariki ni mtu aliyebarikiwa
naye yule unayemlaani, amelaaniwa."[k]

7 Basi wanaume wazee wa
Moabu na wanaume wazee wa
Midiani wakasafiri wakiwa
na malipo ya uaguzi[l] mikononi
mwao nao wakaenda kwa Balaamu[m] na kumwambia maneno ya
Balaki. **8** Ndipo akawaambia:
"Kaeni hapa usiku wa leo, nami
nitawajibu ninyi kama vile tu Yehova atakavyosema nami."[a] Basi
wakuu wa Moabu wakakaa pamoja na Balaamu.

9 Ndipo Mungu akamjia Balaamu na kusema:[b] "Wanaume hawa walio pamoja nawe ni
nani?" **10** Kwa hiyo Balaamu
akamwambia Mungu wa kweli:
"Balaki[c] mwana wa Sipori, mfalme wa Moabu, amewatuma
kwangu, na kusema, **11** 'Tazama! Watu wanaotoka Misri,
nao wanaifunika dunia kufikia upeo wa macho.[d] Sasa njoo,
uwalaani kwa ajili yangu.[e] Huenda nitaweza kupigana nao
na kuwafukuza.'" **12** Lakini
Mungu akamwambia Balaamu:
"Usiende pamoja nao. Usiwalaani watu hao,[f] kwa maana wamebarikiwa."[g]

13 Kisha Balaamu akaondoka asubuhi na kuwaambia wakuu wa Balaki: "Nendeni katika nchi yenu, kwa sababu Yehova amekataa kuniruhusu niende pamoja nanyi." **14** Kwa
hiyo wakuu wa Moabu wakaondoka, wakamjia Balaki na kusema: "Balaamu amekataa kuja
pamoja nasi."[h]

15 Hata hivyo, Balaki akatuma tena wakuu wengine, wengi zaidi na wenye kuheshimika zaidi kuliko wale wa kwanza. **16** Nao wakaja kwa Balaamu na kumwambia: "Hivi
ndivyo ambavyo Balaki mwana
wa Sipori amesema, 'Tafadhali, usizuiliwe kuja kwangu.
17 Kwa maana hakika nitakuheshimu wewe sana,[i] na kila
kitu ambacho utaniambia nitafanya.[j] Kwa hiyo njoo, tafadhali. Walaani watu hawa kwa ajili
yangu.'" **18** Lakini Balaamu
akajibu na kuwaambia watumishi wa Balaki: "Hata kama Balaki angenipa nyumba yake iki-

SURA 22
a Hes 33:48
b Yos 24:9
Amu 11:25
c Kut 15:15
Kum 2:25
d Hes 31:8
Yos 13:21
e Mik 6:5
Ufu 2:14
f Yos 13:22
Yos 24:9
2Pe 2:15
Yud 11
g Kum 23:4
h Mwa 15:18
i Mwa 13:16
j Mwa 12:3
Hes 23:7
Yos 24:9
Ne 13:2
k Zb 109:28
l Mik 3:11
Mdo 16:16
1Ti 6:10
m 2Pe 2:15
Yud 11

Safu ya 2
a Hes 12:6
Hes 23:12
b Hes 22:20
c Hes 22:4
d Hes 22:5
e Hes 22:6
Hes 23:7
Hes 23:11
Hes 24:10
f Mik 6:5
g Mwa 12:2
Mwa 22:17
Hes 23:20
Kum 23:5
Kum 33:29
h Hes 22:37
i Hes 24:11
Met 17:23
j Met 15:27

wa imejaa fedha na dhahabu, singeweza kupita agizo la Yehova
Mungu wangu, ili kufanya ja-
mbo dogo au kubwa.[a] **19** Basi
sasa ninyi pia kaeni hapa, tafa-
dhali, usiku wa leo nipate kujua
Yehova ataniambia nini zaidi.”[b]
20 Ndipo Mungu akamjia
Balaamu usiku na kumwambia:
“Ikiwa wanaume hao wameku-
ja kukuita, ondoka, nenda pa-
moja nao. Lakini neno nitaka-
losema nawe ndilo tu utaka-
losema.”[c] **21** Kisha Balaamu
akaondoka asubuhi, akamta-
ndika punda-jike wake, akaen-
da pamoja na wakuu wa Mo-
abu.[d]
22 Nayo hasira ya Mungu
ikaanza kuwaka kwa sababu
alikuwa akienda; na malaika
wa Yehova akasimama barabarani ili kumzuia.[e] Naye aliku-
wa amepanda juu ya punda-
jike wake, na watumishi wake
wawili walikuwa pamoja naye.
23 Na yule punda akamwona
malaika wa Yehova akiwa
amesimama barabarani, upa-
nga wake uliochomolewa ukiwa mkononi mwake;[f] na yule
punda akajaribu kugeuka ka-
ndo kutoka barabarani aende
shambani, lakini Balaamu aka-
anza kumpiga punda ili kumge-
uza na kumrudisha barabarani.
24 Naye malaika wa Yehova
akaendelea kusimama katika
hiyo njia nyembamba katika-
ti ya mashamba ya mizabibu,
yenye ukuta wa mawe upande
huu na ukuta wa mawe upa-
nde ule. **25** Naye punda-jike
huyo akaendelea kumwona ma-
laika wa Yehova na kuanza ku-
jifinyia ukutani na hivyo kuufi-
nya mguu wa Balaamu ukuta-
ni; naye akazidi kumpiga.
26 Sasa malaika wa Yehova
akapita tena na kusimama ma-

SURA 22
a Hes 24:13
b Hes 22:8
c Hes 22:35
Hes 23:12
Hes 24:13
d Yak 1:14
2Pe 2:15
Yud 11
e Kut 23:21
f 2Fa 6:17
1Nya 21:16

Safu ya 2
a Met 14:16
Met 27:4
b Mt 19:26
2Pe 2:16
c Hes 22:32
d Met 12:10
e 2Pe 2:16
f 2Fa 6:17
g Hes 22:12
Kum 23:4
Mhu 9:3
2Pe 2:15
h Hes 22:23
Hes 22:25
Hes 22:27
i Met 16:25

hali pembamba, ambapo hapa-
kuwa na njia ya kugeuka ku-
ume wala kushoto. **27** Punda
huyo alipomwona malaika wa
Yehova akalala chini, chini ya
Balaamu; hivi kwamba hasi-
ra ya Balaamu ikawaka,[a]
naye akaendelea kumpiga pu-
nda kwa fimbo yake. **28** Mwi-
showe Yehova akafungua ki-
nywa cha punda[b] huyo naye
akamwambia Balaamu: “Ni-
mekutendea nini hivi kwamba
umenipiga mara tatu hizi?”[c]
29 Ndipo Balaamu akamwa-
mbia punda huyo: “Ni kwa sa-
babu umenitendea bila huru-
ma. Laiti ningalikuwa na upa-
nga mkononi mwangu, kufikia
sasa ningalikuwa nimekuua!”[d]
30 Kisha yule punda-jike aka-
mwambia Balaamu: “Je, mimi
si punda wako ambaye ume-
panda maisha yako yote mpa-
ka leo hii? Je, nimezoea ku-
kutendea hivi?”[e] Akajibu: “Ha-
pana!” **31** Na Yehova akafu-
ngua macho[f] ya Balaamu, naye
akamwona malaika wa Yeho-
va amesimama katika barabara na upanga wake uliochomo-
lewa ukiwa mkononi mwake.
Mara moja akainama chini na
kujilaza kifudifudi.
32 Ndipo malaika wa Yehova
akamwambia: “Kwa nini ume-
mpiga punda wako mara hizi
tatu? Tazama! Mimi—mimi ni-
mekuja kukuzuia, kwa sababu
njia yako imekwenda moja kwa
moja kinyume cha mapenzi ya-
ngu.[g] **33** Naye punda aliniona na kujaribu kugeuka kando
mbele yangu mara tatu hizi.[h]
Tuseme asingekuwa amegeu-
ka kando kutoka mbele yangu!
Kufikia sasa ningekuwa nime-
kuua,[i] lakini yeye ningemhi-
fadhi hai.” **34** Ndipo Balaa-
mu akamwambia malaika wa

Yehova: "Nimetenda dhambi,[a]
kwa sababu sikujua kwamba
ni wewe uliyekuwa umesimama
barabarani ili kukutana nami.
Basi sasa, ikiwa ni vibaya ma-
choni pako, acha nirudi zangu."
35 Lakini malaika wa Yehova
akamwambia Balaamu: "Nenda
pamoja na wanaume hao;[b] nawe
hutasema lolote isipokuwa lile
neno nitakalokuambia."[c] Naye
Balaamu akaendelea kwenda
pamoja na wakuu wa Balaki.

36 Balaki aliposikia kwa-
mba Balaamu amekuja, mara
moja akatoka ili kumpokea ka-
tika jiji la Moabu, lililo kwenye
ukingo wa Arnoni, lililo mwi-
shoni mwa eneo hilo.[d] **37** Ndi-
po Balaki akamwambia Bala-
amu: "Je, kwa kweli sikutuma
watu wakuite? Kwa nini huku-
ja kwangu? Je, kwa kweli mimi
siwezi kukuheshimu wewe
kwelikweli?"[e] **38** Basi Balaa-
mu akamwambia Balaki: "Taza-
ma, nimekuja kwako sasa. Je,
nitaweza kusema jambo fula-
ni?[f] Neno ambalo Mungu ata-
tia kinywani mwangu ndilo ni-
takalosema."[g]

39 Kwa hiyo Balaamu akaen-
da pamoja na Balaki nao wa-
kafika Kiriath-husothi. **40** Na
Balaki akatoa dhabihu ng'ombe
na kondoo[h] na kupeleka sehe-
mu yake kwa Balaamu na wale
wakuu waliokuwa pamoja naye.
41 Na ikawa kwamba asubu-
hi Balaki akamchukua Balaamu
na kumleta mpaka Bamoth-baa-
li,[i] ili kutoka huko awaone watu
wote.[j]

23 Kisha Balaamu aka-
mwambia Balaki: "Nije-
ngee mahali hapa madhabahu
saba[k] na unitayarishie maha-
li hapa ng'ombe-dume saba na
kondoo-dume saba." **2** Balaki
akafanya mara moja kama vile
Balaamu alivyokuwa amesee-
ma. Kisha Balaki na Balaamu
wakatoa ng'ombe-dume mmoja
na kondoo-dume mmoja juu ya
kila madhabahu.[a] **3** Na Bala-
amu akamwambia Balaki: "Si-
mama kando ya toleo lako la
kuteketezwa,[b] nami niende. La-
bda Yehova atawasiliana nami
na kukutana nami.[c] Ndipo lolo-
te atakalonionyesha, hakika ni-
takuambia." Basi akaenda kwe-
nye kilima kilicho wazi.

4 Mungu alipowasiliana na
Balaamu,[d] Balaamu akamwa-
mbia: "Niliweka madhabahu
saba katika mistari, nami ni-
katoa ng'ombe-dume mmoja na
kondoo-dume mmoja juu ya kila
madhabahu."[e] **5** Basi Yeho-
va akatia neno katika kinywa
cha Balaamu[f] na kusema: "Rudi
kwa Balaki, na hili ndilo utaka-
losema."[g] **6** Basi akarudi kwa-
ke, na, tazama! yeye na wakuu
wote wa Moabu walikuwa wa-
mesimama kando ya toleo lake
la kuteketezwa. **7** Kisha akaa-
nza neno lake la kimethali[h] na
kusema:

"Kutoka Aramu[i] Balaki
mfalme wa Moabu
alijaribu kuniongoza,
Kutoka katika milima ya
mashariki:
'Njoo, mlaani Yakobo kwa
ajili yangu.
Naam, njoo, washutumu
Israeli.'[j]
8 Ningewezaje kuwalaani
wale ambao Mungu
hajawalaani?[k]
Nami ningewezaje
kuwashutumu wale
ambao Yehova
hajawashutumu?[l]
9 Kwa maana kutoka juu ya
miamba nawaona wao,

SURA 22
a 1Sa 15:24
b Zb 81:12
c Hes 22:20
d Hes 21:26
e Hes 22:17
Hes 24:11
f Met 19:21
g Hes 23:26
Hes 24:13
h Hes 23:14
i Yos 13:15
Yos 13:17
j Hes 23:13

SURA 23
k Hes 22:41

Safu ya 2
a Hes 23:14
Hes 23:30
b Hes 23:15
c Hes 23:16
Hes 24:1
d Hes 22:20
e Hes 23:2
f Hes 22:35
g Hes 23:3
h Hes 23:18
Hes 24:3
i Mwa 10:22
Hes 22:5
Kum 23:4
j Hes 22:6
k Hes 22:12
Hes 24:10
l Met 21:30

Na kutoka vilimani
nawatazama wao.
Wakiwa kikundi cha
watu wanaendelea kukaa
wakiwa wamejitenga,[a]
Nao hawajihesabu katikati
ya mataifa.[b]
10 Ni nani ambaye amehesabu
chembe za mavumbi ya
Yakobo[c]
Na ni nani ambaye
amehesabu sehemu ya
nne ya Israeli?
Nafsi yangu na ife kifo cha
wanyoofu,[d]
Na mwisho wangu na
uwe kama ule wao
mwishowe."[e]

11 Hapo Balaki akamwambia Balaamu: "Umenitendea nini? Nilikuchukua ili uwalaani adui zangu, na, tazama, umewabariki kwelikweli."[f] **12** Naye akajibu na kusema: "Je, lolote ambalo Yehova ametia katika kinywa changu silo ninalopaswa kuwa mwangalifu kulisema?"[g]

13 Ndipo Balaki akamwambia: "Njoo, tafadhali, pamoja nami mpaka mahali pengine ambapo unaweza kuwaona. Ila utauona mwisho wao tu, nawe hutawaona[h] wote. Nawe uwalaani kwa ajili yangu kutoka huko."[i] **14** Basi akampeleka mpaka uwanja wa Sofimu, mpaka juu ya Pisga,[j] na kujenga madhabahu saba na kutoa ng'ombe-dume mmoja na kondoo-dume mmoja juu ya kila madhabahu.[k] **15** Kisha akamwambia Balaki: "Simama hapa kando ya toleo lako la kuteketezwa, na mimi nami acha niwasiliane naye pale." **16** Basi Yehova akawasiliana na Balaamu na kutia neno katika kinywa chake na kusema:[l] "Rudi kwa Balaki,[m] na hili ndilo utakalosema." **17** Basi akaja kwake, na, tazama! alikuwa amesimama kando ya toleo lake la kuteketezwa, na wakuu wa Moabu pamoja naye. Ndipo Balaki akamwambia: "Yehova amesema nini?" **18** Basi akaanza neno lake la kimethali na kusema:[a]

"Ondoka, Balaki, usikilize.
Tega sikio kwangu, Ee
mwana wa Sipori.[b]
19 Mungu si mwanadamu
kwamba aseme uwongo,[c]
Wala si mwana
wa binadamu kwamba
ajute.[d]
Je, yeye mwenyewe
amelisema naye
hatalitenda,
Na je, yeye amesema naye
hatalitimiza?[e]
20 Tazama! nimechukuliwa
nibariki,
Na Yeye amebariki,[f] wala
sitaigeuza.[g]
21 Hajatazama nguvu zozote
za uchawi[h] juu ya Yakobo,
Wala hajaona taabu yoyote
juu ya Israeli.
Yehova Mungu wake yuko
pamoja naye,[i]
Na sauti ya mfalme iko
katikati yake.
22 Mungu anawaleta kutoka
Misri.[j]
Mwendo mwepesi kama
ule wa ng'ombe-dume wa
mwituni ni wake.[k]
23 Kwa maana hakuna apizo
lolote la bahati mbaya
juu ya Yakobo,[l]
Wala uaguzi wowote juu ya
Israeli.[m]
Na wakati huu inaweza
kusemwa juu ya Yakobo
na Israeli,
'Mungu ametenda nini!'[n]

SURA 23

a Law 20:24
Kum 33:28
1Fa 8:53
Est 3:8
b Kut 33:16
Kum 32:8
c Mwa 13:16
Mwa 22:17
Kut 1:7
d Zb 37:37
Zb 116:15
Met 10:7
e Yos 14:14
Isa 26:19
1Ko 15:55
Ebr 11:35
f Hes 22:11
Hes 24:10
Yos 24:10
Ne 13:2
Zb 109:28
Mik 6:5
g Hes 22:38
Hes 24:13
h Hes 22:11
i Yos 24:9
j Kum 34:1
k Hes 23:1
Hes 23:29
l Hes 22:35
Hes 23:5
Hes 24:1
m Hes 22:10

Safu ya 2

a Hes 23:7
Hes 24:3
b Hes 22:2
Yos 24:9
c Zb 89:35
Tit 1:2
d 1Sa 15:29
Ro 11:29
e Isa 14:24
Isa 46:10
Mik 7:20
f Mwa 12:2
Mwa 22:17
Hes 22:12
g Hes 22:18
Mal 3:6
h 1Sa 15:23
i Kut 13:21
Kut 23:20
Kut 29:45
Kut 34:9
Isa 8:10
j Kut 20:2
k Hes 24:8
l Mwa 12:3
Hes 22:6
m Hes 22:7
Kum 18:10
Kum 18:12
n Zb 31:19
Zb 44:1
Zb 126:3
Ro 11:33

24 Tazama, kikundi cha watu
kitasimama kama simba,
Na kama simba kitajiinua.[a]
Hakitalala chini mpaka
kile mawindo,
Na damu ya waliouawa
kitakunywa."[b]
25 Hapo Balaki akamwambia
Balaamu: "Ikiwa, kwa upande
mmoja, huwezi kumlaani hata
kidogo, basi, kwa upande mwi-
ngine, hupaswi kumbariki hata
kidogo." **26** Naye Balaamu
akajibu na kumwambia Balaki:
"Je, sikusema nawe, na kukua-
mbia, 'Yote ambayo Yehova ata-
sema ndiyo nitakayotenda'?"[c]
27 Ndipo Balaki akamwa-
mbia Balaamu: "Njoo, tafa-
dhali. Acha nikupeleke maha-
li pengine tena. Labda itaku-
wa sawa machoni pa Mungu
wa kweli ili upate kuwalaani
kwa ajili yangu kutoka huko."[d]
28 Kwa hiyo Balaki akamchu-
kua Balaamu mpaka juu ya
Peori, unaoelekea Yeshimoni.[e]
29 Kisha Balaamu[f] akamwa-
mbia Balaki: "Nijengee mahali
hapa madhabahu saba na unita-
yarishie mahali hapa ng'ombe-
dume saba na kondoo-dume
saba."[g] **30** Basi Balaki akafa-
nya kama vile Balaamu alivyo-
kuwa amesema, naye akatoa
ng'ombe-dume mmoja na ko-
ndoo-dume mmoja kwenye kila
madhabahu.[h]

24 Balaamu alipoona kwa-
mba ilikuwa vema ma-
choni pa Yehova kubariki Israe-
li, hakuenda kama zile mara
nyingine[i] na kutafuta ishara
zozote za bahati mbaya,[j] bali
alielekeza uso wake nyikani.
2 Balaamu alipoinua macho
yake na kumwona Israeli aki-
kaa kulingana na makabila
yake,[a] ndipo roho ya Mungu ika-
ja juu yake.[b] **3** Basi akaanza
neno lake la kimethali[c] na ku-
sema:
"Neno la Balaamu mwana
wa Beori,
Na neno la
mwanamume jicho likiwa
limefunguliwa,[d]
4 Neno la mtu anayesikia
maneno ya Mungu,[e]
Aliyeona maono ya
Mweza-Yote[f]
Alipokuwa akianguka
chini macho yakiwa
yamefunguliwa:[g]
5 Ni yenye kupendeza kama
nini mahema yako, Ee
Yakobo, maskani zako,
Ee Israeli![h]
6 Yameenea mbali kama
mabonde ya mto,[i]
Kama bustani kando ya
mto.[j]
Kama mimea ya
udi ambayo Yehova
amepanda,
Kama mierezi kando ya
maji.[k]
7 Maji yanatiririka kutoka
katika ndoo zake mbili za
ngozi,
Na mbegu yake iko kando
ya maji mengi.[l]
Mfalme[m] wake pia atakuwa
juu kuliko Agagi,[n]
Na ufalme wake utainuliwa
juu.[o]
8 Mungu anamleta kutoka
Misri;
Ule mwendo mwepesi
wa ng'ombe-dume wa
mwituni ni wake.[p]
Atayateketeza mataifa,
wakandamizaji wake,[q]
Na mifupa yao
ataitafuna-tafuna,[r] naye
atawavunja

SURA 23
a Mwa 49:9
Hes 24:9
Met 30:30
b Isa 31:4
Mik 5:8
c Hes 22:38
Hes 23:12
Hes 24:13
d Hes 23:13
e Hes 21:20
f Hes 22:5
g Hes 23:1
h Hes 23:2
Hes 23:14

SURA 24
i Hes 23:3
Hes 23:15
j Mwa 30:27
Law 19:26
Hes 23:23

Safu ya 2
a Hes 2:2
Hes 23:9
b Hes 11:25
1Sa 19:20
2Nya 15:1
1Ko 12:10
c Hes 23:7
d Amo 3:7
e Hes 24:16
f Hes 12:6
g Eze 1:28
h Hes 1:52
Hes 2:2
i Hes 2:32
Hes 22:11
j Isa 58:11
Yer 31:12
k Zb 1:3
Zb 92:12
Yer 17:8
l Kum 8:7
m Mwa 49:10
Zb 2:6
Yoh 1:49
Flp 2:10
Ufu 19:16
n Hes 24:20
o 1Nya 14:2
Da 2:44
Mdo 5:31
Ufu 11:15
p Hes 23:22
q Kut 23:27
Kum 9:5
Ufu 19:15
r Isa 38:13

vipande-vipande kwa
mishale yake.[a]
9 Aliinama chini, akalala
kama simba,
Na, kama simba, ni nani
anayethubutu
kumwamsha?[b]
Wale wanaokubariki ndio
waliobarikiwa,[c]
Nao wale wanaokulaani
ndio waliolaaniwa."[d]

10 Ndipo hasira ya Balaki ikawaka juu ya Balaamu naye akapiga makofi,[e] naye Balaki akamwambia Balaamu: "Nilikuita ili uwalaani[f] adui zangu, na, tazama! umewabariki kabisa mara hizi tatu. **11** Basi sasa kimbia uende kwako. Nilikuwa nimesema moyoni mwangu kwamba nitakuheshimu wewe,[g] lakini, tazama! Yehova amekuzuilia usipate heshima."

12 Naye Balaamu akamwambia Balaki: "Je, sikuwaambia wajumbe wako uliowatuma kwangu na kusema, **13** 'Hata ikiwa Balaki angenipa nyumba yake iliyojaa fedha na dhahabu, singeweza kupita agizo la Yehova na kufanya jambo jema au baya kutoka moyoni mwangu mwenyewe. Lolote lile ambalo Yehova atasema ndilo nitakalosema'?[h] **14** Na sasa, tazama, naenda zangu kwa watu wangu. Njoo, acha nikushauri[i] wewe mambo ambayo watu hawa watawatendea watu wako baadaye katika siku za mwisho."[j] **15** Kwa hiyo akaanza neno lake la kimethali[k] na kusema:

"Neno la Balaamu mwana
wa Beori,
Na neno la
mwanamume jicho likiwa
limefunguliwa,[l]

SURA 24

a Kum 32:42
Zb 2:9
b Mwa 49:9
c Mwa 12:3
d Mwa 27:29
e Ayu 27:23
Nah 3:19
f Hes 22:11
Hes 23:11
Kum 23:4
Yos 24:9
Ne 13:2
g Hes 22:17
Yud 11
h Hes 22:18
Hes 22:38
i Mik 6:5
j Yer 48:46
k Hes 23:7
Hes 24:3
l Hes 24:3

Safu ya 2

a Hes 24:4
b Hes 12:6
c Eze 1:28
d Kut 33:20
Yoh 1:18
e 2Sa 7:16
Isa 9:7
Isa 14:13
Yer 23:5
Eze 21:27
2Pe 1:19
Ufu 22:16
f Mwa 49:10
Zb 45:6
Zb 108:8
Zb 110:2
Ebr 1:8
g 2Sa 8:2
1Nya 18:2
Zb 108:9
Zb 110:6
Yer 48:45
h Mwa 27:37
2Sa 8:14
1Nya 18:13
Zb 60:8
Isa 34:5
Amo 9:12
i Mwa 36:8
Yos 24:4
j 1Nya 4:42
Eze 25:14
k Mwa 49:10
Zb 2:9
Zb 72:11
Ufu 6:2
Ufu 19:15
l Ufu 19:21
m Hes 23:7
n Kut 17:8
Kut 17:14
o Kum 25:19
1Sa 15:3
1Nya 4:43
p Mwa 15:19
Amu 1:16
q Amu 4:11

16 Neno la yule anayesikia
maneno ya Mungu,[a]
Na yule anayejua ujuzi wa
Aliye Juu Zaidi—
Maono ya Mweza-Yote
aliyaona[b]
Alipokuwa akianguka
chini macho yake yakiwa
yamefunguliwa:[c]
17 Nitamwona,[d] bali si sasa;
Nitamtazama, bali si
karibu.
Nyota[e] itatokea katika
Yakobo,
Na fimbo ya enzi itainuka
katika Israeli.[f]
Naye atavunja vipaji vya
kichwa cha Moabu[g]
Na fuvu la kichwa cha
wana wote wa fujo ya
vita.
18 Na Edomu itakuwa miliki,[h]
Naam, Seiri[i] itakuwa miliki
ya adui zake,[j]
Huku Israeli akionyesha
uhodari wake.
19 Na kutoka katika Yakobo
mtu ataenda akitiisha,[k]
Naye atamharibu
mwokokaji yeyote
kutoka katika jiji."[l]

20 Alipomwona Amaleki, akaendeleza neno lake la kimethali na kusema:[m]
"Amaleki alikuwa wa
kwanza wa mataifa,[n]
Lakini mwisho wake
baadaye utakuwa
kuangamia kwake."[o]

21 Alipowaona Wakeni,[p] akaendeleza neno lake la kimethali na kuendelea kusema:
"Makao yako ni yenye
kudumu, na makao yako
yamewekwa juu ya
mwamba.
22 Lakini kutakuwa na mtu
wa kuteketeza Kayini.[q]

Itachukua muda mrefu
kadiri gani mpaka
Ashuru
atakapokuchukua
mateka?"[a]

23 Naye akaendeleza neno
lake la kimethali na kuendelea
kusema:
"Ole! Ni nani atakayeokoka
wakati Mungu
atakapolisababisha?[b]
24 Na kutakuwako meli
kutoka pwani ya Kitimu,[c]
Nazo hakika zitatesa
Ashuru,[d]
Nazo zitatesa Eberi
kwelikweli.
Lakini yeye pia
ataangamia mwishowe."

25 Kisha Balaamu akaondoka, akaenda na kurudi kwake.[e] Na Balaki pia akaenda zake.

25 Sasa Israeli alikuwa akikaa Shitimu.[f] Ndipo watu wakaanza kufanya uasherati na binti za Moabu.[g] **2** Na wanawake hao wakaja kuwaita watu waende kwenye dhabihu za miungu yao,[h] nao watu wakaanza kula na kuinamia miungu yao.[i] **3** Kwa hiyo Israeli akajishikamanisha na Baali wa Peori;[j] nayo hasira ya Yehova ikaanza kuwaka juu ya Israeli.[k] **4** Basi Yehova akamwambia Musa: "Chukua wote walio vichwa vya watu nawe uwaanike mbele za Yehova kuelekea jua, ili hasira inayowaka ya Yehova[l] igeukie mbali na Israeli." **5** Ndipo Musa akawaambia waamuzi wa Israeli:[m] "Kila mmoja wenu awaue[n] watu wake ambao wameshikamana na Baali wa Peori."

6 Lakini, tazama! mwanamume[o] mmoja kati ya wana wa Israeli akaja, naye alikuwa akimleta mwanamke Mmidiani[p] karibu na ndugu zake, mbele ya macho ya Musa na mbele ya macho ya kusanyiko lote la wana wa Israeli, walipokuwa wakilia kwenye mwingilio wa hema la mkutano. **7** Finehasi[a] mwana wa Eleazari mwana wa Haruni kuhani alipoona hilo, akainuka mara moja kutoka katikati ya kusanyiko, akachukua mkuki mkononi mwake. **8** Kisha akamfuata yule mwanamume wa Israeli ndani ya hema lenye kuba na kuwachoma wote wawili, mwanamume huyo wa Israeli na mwanamke huyo kupitia sehemu zake za uzazi. Ndipo tauni ikakomeshwa kutoka kwa wana wa Israeli.[b] **9** Nao waliokufa kutokana na tauni hiyo walijumlika kuwa 24,000.[c]

10 Kisha Yehova akasema na Musa, na kumwambia: **11** "Finehasi[d] mwana wa Eleazari mwana wa Haruni kuhani ameigeuzia mbali ghadhabu[e] yangu kutoka juu ya wana wa Israeli kwa kutovumilia kwake ushindani wowote kunielekea mimi katikati yao,[f] hivi kwamba sikuwaangamiza wana wa Israeli kwa kusisitiza kwangu kwamba watu wajitoe kikamili.[g] **12** Kwa sababu hiyo, 'Tazama, nampa yeye agano langu la amani. **13** Nalo litatumika kama agano la ukuhani mpaka wakati usio na kipimo kwa ajili yake na uzao wake baada yake,[h] kwa kuwa hakuvumilia ushindani wowote kumwelekea Mungu[i] wake naye alifanya upatanisho kwa ajili ya wana wa Israeli.'"[j]

14 Jina la mwanamume huyo Mwisraeli aliyepigwa na kuuawa pamoja na yule mwanamke Mmidiani lilikuwa Zi-

SURA 24
a 2Fa 15:29; Ezr 4:2
b Kum 32:39
c Mwa 10:4; Isa 23:1; Eze 27:6; Da 11:30
d Nah 1:1; Nah 3:18
e Hes 31:8

SURA 25
f Yos 2:1; Mik 6:5
g Hes 31:16; 1Ko 10:8; Ufu 2:14
h Kut 34:15; 1Fa 11:2; Mdo 15:29; 1Ko 10:20
i Kut 20:5; Yos 23:7; 1Ko 10:7
j Kum 4:3; Yos 22:17; Zb 106:28; Ho 9:10
k Zb 106:29
l 2Sa 21:6
m Kut 18:21
n Kut 22:20; Kut 32:27; Kum 13:8; Kum 13:9; 1Fa 18:40
o Hes 25:14
p Hes 25:15

Safu ya 2
a Kut 6:25; Yos 22:30; 1Nya 6:4
b Kut 23:21; Zb 106:30
c Hes 25:4; Kum 4:3; 1Ko 10:8
d Hes 25:7
e Zb 106:30
f Zb 106:31; 2Ko 11:2
g Kut 20:5; Kut 34:14; Kum 4:24; Yos 24:19
h 1Nya 6:4; 1Nya 6:50; Ezr 7:5; Ezr 8:2
i 1Fa 19:10
j Kut 32:30

mri mwana wa Salu, mkuu[a] wa
nyumba ya ukoo wa upande wa
baba ya Wasimeoni. **15** Nalo
jina la mwanamke Mmidiani
aliyepigwa na kuuawa lilikuwa
Kozbi binti ya Suri;[b] huyo aliku-
wa kichwa katika ukoo wa nyu-
mba ya upande wa baba yake
katika Midiani.[c]

16 Baadaye Yehova akasema
na Musa, na kumwambia:
17 "Wamidiani na wasumbuli-
we, nanyi mtawapiga,[d] **18** kwa
sababu wanawasumbua ninyi
kwa matendo yao ya ujanja[e]
ambayo wamewatendea ninyi
kwa ujanja katika lile jambo la
Peori[f] na katika lile jambo la
Kozbi[g] binti ya mkuu wa Mi-
diani, dada yao ambaye alipi-
gwa na kuuawa[h] katika ile siku
ya tauni kuhusu lile jambo la
Peori."[i]

26 Na ikawa kwamba baa-
da ya tauni hiyo,[j] Yeho-
va akamwambia hivi Musa na
Eleazari mwana wa Haruni ku-
hani: **2** "Chukueni hesabu ya
kusanyiko lote la wana wa Isra-
eli kuanzia umri wa miaka 20
na zaidi, kulingana na nyumba
ya baba zao, wale wote wana-
oingia jeshini katika Israeli."[k]
3 Naye Musa na Eleazari[l] ku-
hani wakaanza kusema nao ka-
tika nchi tambarare za jangwa
la Moabu[m] kando ya Mto Yorda-
ni huko Yeriko,[n] na kuwaambia:
4 "Chukueni hesabu yao kua-
nzia umri wa miaka 20 na zai-
di, kama vile Yehova alivyoku-
wa amemwamuru Musa."[o]

Sasa wana wa Israeli walio-
toka nchi ya Misri walikuwa:
5 Rubeni, mzaliwa wa kwanza[p]
wa Israeli; wana wa Rubeni:
Wa Hanoki[q] familia ya Wahano-
ki; wa Palu[r] familia ya Wapalu;
6 wa Hezroni[s] familia ya Wahe-
zroni; wa Karmi[a] familia ya Wa-
karmi. **7** Hizo ndizo zilizoku-
wa familia za Warubeni, nao
walioandikishwa kati yao wali-
jumlika kuwa 43,730.[b]

8 Na mwana wa Palu aliku-
wa Eliabu. **9** Nao wana wa
Eliabu: Nemueli na Dathani
na Abiramu. Dathani[c] huyu na
Abiramu[d] walikuwa watu wali-
oitwa na kusanyiko, ambao wa-
lipambana na Musa na Haruni
katika kusanyiko la Kora,[e] wa-
lipopambana na Yehova.

10 Ndipo dunia ikafungua
kinywa chake na kuwameza.[f]
Naye Kora, alikufa kwenye kifo
cha kusanyiko wakati amba-
po moto uliwateketeza watu
250.[g] Nao wakaja kuwa mfano.[h]
11 Hata hivyo, wana wa Kora
hawakufa.[i]

12 Wana wa Simeoni[j] kuli-
ngana na familia zao: wa Nemu-
eli[k] familia ya Wanemueli; wa
Yamini[l] familia ya Wayamini;
wa Yakini[m] familia ya Wayakini;
13 wa Zera familia ya Wazera;
wa Shauli[n] familia ya Washauli.
14 Hizo ndizo zilizokuwa fami-
lia za Wasimeoni: 22,200.[o]

15 Wana wa Gadi[p] kulingana
na familia zao: Wa Sefoni fami-
lia ya Wasefoni; wa Hagi fami-
lia ya Wahagi; wa Shuni familia
ya Washuni; **16** wa Ozni fami-
lia ya Waozni; wa Eri familia
ya Waeri; **17** wa Arodi fami-
lia ya Waarodi; wa Areli[q] fami-
lia ya Waareli. **18** Hizo ndizo
zilizokuwa familia za wana wa
Gadi, za walioandikishwa kati
yao: 40,500.[r]

19 Wana wa Yuda[s] walikuwa
Eri[t] na Onani.[u] Hata hivyo, Eri
na Onani walikufa katika nchi
ya Kanaani.[v] **20** Nao wana
wa Yuda wakawa, kulingana na
familia zao: Wa Shela[w] familia

SURA 25

a Hes 1:16
b Hes 31:8
Yos 13:21
c Mwa 25:2
1Nya 1:32
d Hes 31:2
e Hes 31:16
2Pe 2:14
Ufu 2:14
f Hes 25:3
Ne 13:2
2Pe 2:15
Yud 11
g Hes 25:15
h Hes 25:8
i Hes 25:9

SURA 26

j Hes 25:5
Hes 25:8
k Kut 30:12
Kut 38:26
Hes 1:2
l Hes 20:26
m Hes 22:1
Hes 31:12
Hes 33:48
n Kum 34:3
Yos 6:1
o Hes 1:3
p Mwa 29:32
Mwa 46:8
1Nya 5:1
q Kut 6:14
r Mwa 46:9
s 1Nya 5:3

Safu ya 2

a Kut 6:14
b Hes 1:21
c Hes 16:24
Kum 11:6
d Hes 16:1
Hes 16:12
Hes 16:27
Zb 106:17
e Hes 16:5
Hes 16:19
Yud 11
f Hes 16:32
g Hes 16:35
Zb 106:18
h Hes 16:38
Eze 14:8
1Ko 10:11
2Pe 2:6
i Kut 6:24
Hes 26:58
Zb 42:Uta
Zb 45:Uta
j Mwa 35:23
Mwa 46:10
k Mwa 46:10
l 1Nya 4:24
m Kut 6:15
n 1Nya 4:24
o Hes 1:23
p Mwa 35:26
q Mwa 46:16
r Hes 1:25
s Mwa 29:35
Mwa 49:10
1Nya 5:2
Ebr 7:14
t Mwa 38:3
u Mwa 38:4
1Nya 2:3
v Mwa 38:7
Mwa 38:9
Mwa 38:10
w Mwa 38:5
Mwa 38:26
1Nya 4:21

ya Washela; wa Perezi[a] familia ya Waperezi; wa Zera[b] familia ya Wazera. **21** Nao wana wa Perezi wakawa: Wa Hezroni[c] familia ya Wahezroni; wa Hamuli[d] familia ya Wahamuli. **22** Hizo ndizo zilizokuwa familia za Yuda,[e] za walioandikishwa kati yao: 76,500.[f]

23 Wana wa Isakari[g] kulingana na familia zao walikuwa: Wa Tola[h] familia ya Watola; wa Puva familia ya Wapuni; **24** wa Yashubu familia ya Wayashubu; wa Shimroni[i] familia ya Washimroni. **25** Hizo ndizo zilizokuwa familia za Isakari, za walioandikishwa kati yao: 64,300.[j]

26 Wana wa Zabuloni[k] kulingana na familia zao walikuwa: Wa Seredi familia ya Waseredi; wa Eloni familia ya Waeloni; wa Yahleeli[l] familia ya Wayahleeli. **27** Hizo ndizo zilizokuwa familia za Wazabuloni, za walioandikishwa kati yao: 60,500.[m]

28 Wana wa Yosefu[n] kulingana na familia zao walikuwa Manase na Efraimu.[o] **29** Wana wa Manase[p] walikuwa: Wa Makiri[q] familia ya Wamakiri. Naye Makiri akamzaa Gileadi.[r] Wa Gileadi familia ya Wagileadi. **30** Hawa ndio waliokuwa wana wa Gileadi: Wa Yezeri[s] familia ya Wayezeri; wa Heleki familia ya Waheleki; **31** wa Asrieli familia ya Waasrieli; wa Shekemu familia ya Washekemu; **32** wa Shemida[t] familia ya Washemida; wa Heferi[u] familia ya Waheferi. **33** Sasa Selofehadi mwana wa Heferi hakuwa na wana, bali binti,[v] na majina ya binti za Selofehadi yalikuwa Mala na Noa, Hogla, Milka na Tirsa.[w] **34** Hizo ndizo zilizokuwa familia za Manase, nao walioandikishwa kati yao walikuwa 52,700.[a]

35 Hawa ndio waliokuwa wana wa Efraimu[b] kulingana na familia zao: Wa Shuthela[c] familia ya Washuthela; wa Bekeri familia ya Wabekeri; wa Tahani[d] familia ya Watahani. **36** Nao hawa ndio wana wa Shuthela: Wa Erani familia ya Waerani. **37** Hizo ndizo zilizokuwa familia za wana wa Efraimu,[e] za walioandikishwa kati yao: 32,500. Hao ndio waliokuwa wana wa Yosefu kulingana na familia zao.[f]

38 Wana wa Benyamini[g] kulingana na familia zao walikuwa: Wa Bela[h] familia ya Wabela; wa Ashbeli[i] familia ya Waashbeli; wa Ahiramu familia ya Waahiramu; **39** wa Shefufamu familia ya Washufamu; wa Hufamu[j] familia ya Wahufamu. **40** Wana wa Bela wakawa Ardi na Naamani:[k] Wa Ardi familia ya Waardi; wa Naamani familia ya Wanaamani. **41** Hao ndio waliokuwa wana wa Benyamini[l] kulingana na familia zao, nao walioandikishwa kati yao walikuwa 45,600.[m]

42 Hawa ndio waliokuwa wana wa Dani[n] kulingana na familia zao: Wa Shuhamu familia ya Washuhamu. Hizo ndizo zilizokuwa familia za Dani[o] kulingana na familia zao. **43** Familia zote za Washuhamu, za walioandikishwa kati yao, walikuwa 64,400.[p]

44 Wana wa Asheri[q] kulingana na familia zao walikuwa: Wa Imna[r] familia ya Waimna; wa Ishvi[s] familia ya Waishvi; wa Beria familia ya Waberia; **45** wa wana wa Beria: Wa Heberi familia ya Waheberi; wa Malkieli[t] familia ya Wamalkieli. **46** Nalo jina la

SURA 26

a Mwa 38:29
Mwa 46:12
Ru 4:18
Mt 1:3
b Mwa 38:30
1Nya 2:4
c Ru 4:19
d Mwa 46:12
1Nya 2:5
e Mwa 49:8
f Hes 1:27
g Mwa 30:18
Mwa 35:23
Mwa 46:13
h 1Nya 7:2
i 1Nya 7:1
j Hes 1:29
k Mwa 30:20
l Mwa 46:14
m Hes 1:31
n Mwa 30:24
Mwa 35:24
o Mwa 41:52
Mwa 46:20
Kum 33:17
p Mwa 41:51
Mwa 48:5
q Mwa 50:23
Hes 36:1
Kum 3:15
1Nya 7:14
r Yos 17:1
s Yos 17:2
t Yos 17:2
u Hes 27:1
v Hes 27:7
Hes 36:2
Yos 17:3
1Nya 7:15
w Hes 27:1
Hes 36:11

Safu ya 2

a Hes 1:35
b Mwa 41:52
c 1Nya 7:20
d 1Nya 7:25
e Mwa 48:20
Yos 17:17
f Hes 1:33
g Mwa 35:24
h 1Nya 7:6
i 1Nya 8:1
j Mwa 46:21
k Mwa 46:21
1Nya 8:7
l Mwa 49:27
Amu 1:21
m Hes 1:37
n Mwa 30:6
o Mwa 49:16
p Hes 1:39
q Mwa 30:13
Mwa 35:26
r Mwa 46:17
s 1Nya 7:30
t Mwa 46:17

binti ya Asheri lilikuwa Sera.[a]
47 Hizo ndizo zilizokuwa familia za wana wa Asheri,[b] za waliondikishwa kati yao: 53,400.[c]

48 Wana wa Naftali[d] kulingana na familia zao walikuwa: Wa Yahzeeli[e] familia ya Wayahzeeli; wa Guni[f] familia ya Waguni;
49 wa Yezeri[g] familia ya Wayezeri; wa Shilemu[h] familia ya Washilemu. **50** Hizo ndizo zilizokuwa familia za Naftali[i] kulingana na familia zao, nao walioandikishwa kati yao walikuwa 45,400.[j]

51 Hawa ndio walioandikishwa kati ya wana wa Israeli: 601,730.[k]

52 Kisha Yehova akasema na Musa, na kumwambia:
53 "Kwa hawa nchi itagawanywa kwa ajili ya urithi kulingana na hesabu ya majina yao.[l]
54 Kulingana na hesabu kubwa utaongeza urithi wa mtu, na kulingana na uchache utapunguza urithi wa mtu.[m] Kila urithi wa mtu utatolewa kulingana na watu wake walioandikishwa. **55** Nchi itagawanywa kwa kura[n] tu. Kulingana na majina ya makabila ya baba zao watapata urithi. **56** Kwa uamuzi wa kura urithi wa mtu utagawanywa kati ya walio wengi na walio wachache."

57 Sasa hawa ndio walioandikishwa wa Walawi[o] kulingana na familia zao: Wa Gershoni[p] familia ya Wagershoni; wa Kohathi[q] familia ya Wakohathi; wa Merari[r] familia ya Wamerari.
58 Hizi ndizo zilizokuwa familia za Walawi: familia ya Walibni,[s] familia ya Wahebroni,[t] familia ya Wamali,[u] familia ya Wamushi,[v] familia ya Wakora.[w]

Na Kohathi[x] akamzaa Amramu.[y] **59** Nalo jina la mke wa Amramu lilikuwa Yokebedi,[z] binti ya Lawi, ambaye mke wake alimzalia Lawi katika Misri. Baada ya muda akamzalia Amramu Haruni na Musa na Miriamu dada yao.[a] **60** Kisha Haruni akazaa Nadabu na Abihu,[b] Eleazari na Ithamari.[c] **61** Lakini Nadabu na Abihu walikufa kwa sababu ya kutoa moto haramu mbele za Yehova.[d]

62 Nao walioandikishwa kati yao wakawa 23,000, wanaume wote kuanzia umri wa mwezi mmoja na zaidi.[e] Kwa maana hawakuandikishwa katikati ya wana wa Israeli,[f] kwa sababu hawakupaswa kupewa urithi wowote katikati ya wana wa Israeli.[g]

63 Hawa ndio walioandikishwa na Musa na Eleazari kuhani walipowaandikisha wana wa Israeli katika nchi tambarare za jangwa la Moabu kando ya Yordani huko Yeriko.[h]
64 Lakini kati ya hao hakukuwa na mtu kati ya wale walioandikishwa na Musa na Haruni kuhani wakati ambapo waliwaandikisha wana wa Israeli katika nyika ya Sinai.[i] **65** Kwa maana Yehova alikuwa amesema hivi juu yao: "Lazima watakufa nyikani."[j] Kwa hiyo hakubaki mtu yeyote kati yao isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune na Yoshua mwana wa Nuni.[k]

27 Ndipo binti za Selofehadi[l] mwana wa Heferi mwana wa Gileadi mwana wa Makiri mwana wa Manase,[m] wa familia za Manase mwana wa Yosefu, wakaja karibu. Na haya ndiyo yaliyokuwa majina ya binti zake: Mala, Noa na Hogla na Milka na Tirsa.[n] **2** Nao

SURA 26
a 1Nya 7:30
b Mwa 49:20 Kum 33:24
c Hes 1:41
d Mwa 30:8 Mwa 35:25
e Mwa 46:24
f 1Nya 7:13
g Mwa 46:24
h 1Nya 7:13
i Mwa 49:21
j Hes 1:43
k Kut 38:26 Hes 1:46 Hes 1:49 Hes 2:32 Hes 14:29 Ne 9:23
l Yos 11:23 Yos 14:1
m Hes 33:54 Yos 17:14
n Hes 34:13 Yos 14:2 Yos 17:4 Yos 18:6 Met 16:33
o Kut 6:19 Hes 3:15 Yos 18:7
p Mwa 46:11 Hes 3:17 Yos 21:6
q Kut 6:16 Hes 3:19 Yos 21:4
r Yos 21:7 1Nya 6:1
s Kut 6:17 Hes 3:18
t Hes 3:27 1Nya 6:2
u Kut 6:19 Hes 3:33 1Nya 23:21
v Hes 3:20 1Nya 23:23
w Kut 6:24 1Nya 6:33 1Nya 6:37
x 1Nya 23:12
y Kut 6:18 Hes 3:19
z Kut 2:1 Kut 6:20

Safu ya 2
a Kut 15:20 Mik 6:4
b Kut 6:23 Kut 24:9 Law 10:1
c Law 10:16 Hes 3:2
d Law 10:2 Hes 3:4 1Nya 24:2
e Hes 3:39
f Hes 1:49
g Hes 18:24 Kum 10:9 Kum 14:27 Yos 14:3
h Hes 26:3
i Hes 1:2 Kum 2:14 1Ko 10:5
j Hes 14:29 Ebr 3:17
k Hes 14:30 Yos 14:14 Yos 19:49

SURA 27 l Hes 26:33; 1Nya 7:15; m Hes 26:28; n Yos 17:3.

wakasimama mbele ya Musa
na mbele ya Eleazari kuhani[a] na mbele ya wakuu na kusanyiko lote kwenye mwingilio wa hema la mkutano, na
kusema: **3** "Baba yetu alikufa nyikani,[b] wala hakuwa katikati ya lile kusanyiko, yaani, wale waliojipanga dhidi
ya Yehova katika kusanyiko la Kora,[c] bali alikufa kutokana na dhambi yake mwenyewe;[d] naye hakuwa na wana wowote wa kiume. **4** Kwa nini jina la baba
yetu liondolewe kutoka katikati ya familia yake kwa sababu hakuwa na mwana?[e] Tupe miliki katikati ya ndugu za baba
yetu."[f] **5** Ndipo Musa akaiweka kesi yao mbele za Yehova.[g]

6 Kisha Yehova akamwambia Musa hivi: **7** "Binti za
Selofehadi wanasema jambo lililo sawa. Wape miliki ya urithi katikati ya ndugu za baba
yao, nawe utaupitisha urithi wa baba yao kwao.[h] **8** Nawe utasema na wana wa Israeli, na kuwaambia, 'Ikiwa mtu yeyote
atakufa bila kuwa na mwana, mtaupitisha urithi wake kwa binti yake. **9** Na ikiwa hana
binti, mtawapa ndugu zake urithi wake. **10** Na ikiwa hana
ndugu, mtawapa ndugu za baba yake urithi wake. **11** Na ikiwa baba yake hana ndugu, mtampa urithi wake mtu wa familia yake aliye wa karibu zaidi
na mwenye uhusiano wa damu,[i] naye atauchukua. Nayo itatumika kama sheria kulingana na
uamuzi wa hukumu kwa ajili ya wana wa Israeli, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.'"

12 Basi Yehova akamwambia
Musa: "Nenda juu katika mlima huu wa Abarimu,[j] ukaone nchi

SURA 27

a Kut 18:26
Kum 17:8
b Hes 14:35
c Hes 16:2
Hes 16:19
Hes 16:35
d Eze 18:4
Ro 5:12
Ro 6:23
e Hes 26:64
f Yos 17:4
g Kut 18:15
Kut 33:11
Law 24:12
h Hes 36:2
Yos 17:6
i Law 25:25
Law 25:49
Ru 4:3
Yer 32:8
j Hes 33:47
Kum 32:49

Safu ya 2

a Mwa 13:15
Kum 3:27
Kum 32:52
Kum 34:1
b Hes 31:2
Kum 34:7
c Hes 20:24
Hes 20:28
Hes 33:38
Kum 10:6
Kum 32:50
d Hes 20:10
Kum 1:37
Zb 106:33
e Hes 20:12
f Zb 106:32
g Kum 1:2
Kum 32:51
h Hes 13:21
Yos 15:1
i Hes 27:18
Zb 31:5
Zb 104:29
j Hes 16:22
Ayu 12:10
k Kum 31:14
l Kum 31:2
m 1Fa 22:17
Mt 9:36
n Hes 14:24
2Fa 2:9
Lu 1:17
o Kum 34:9
Mdo 6:6
1Ti 4:14
p Kum 31:7
q Kum 1:38
Kum 31:3
Kum 34:10
r Yos 1:17
s 1Sa 22:10
1Sa 28:6
t Kut 28:30
Law 8:8
Kum 33:8
1Sa 23:9
1Sa 28:6
Ne 7:65

ambayo hakika nitawapa wana
wa Israeli.[a] **13** Ukiisha kuiona, ndipo utakusanywa kwa watu wako,[b] naam, wewe, kama
vile Haruni ndugu yako alivyokusanywa,[c] **14** kwa sababu ninyi mliasi agizo langu katika nyika ya Zini kusanyiko lilipogombana,[d] juu ya kunitakasa[e] kando ya maji mbele ya
macho yao. Hayo ndiyo maji ya Meriba[f] huko Kadeshi[g] katika nyika ya Zini."[h]

15 Kisha Musa akasema na Yehova, na kumwambia: **16** "Yehova Mungu wa roho[i] za namna
zote za mwili[j] na aweke rasmi juu ya kusanyiko mwanamume[k] **17** ambaye atatoka nje mbele yao na ambaye
ataingia ndani mbele yao na ambaye atawatoa nje na ambaye atawaingiza ndani,[l] ili kusanyiko la Yehova lisiwe kama
kondoo wasio na mchungaji."[m] **18** Kwa hiyo Yehova akamwambia Musa: "Jichukulie Yoshua
mwana wa Nuni, mwanamume ambaye ndani yake mna roho,[n] nawe utaweka mkono wako juu
yake;[o] **19** nawe umsimamishe mbele ya Eleazari kuhani na mbele ya kusanyiko lote, nawe
umpe utume mbele ya macho yao.[p] **20** Nawe utatia sehemu ya utukufu wako juu yake,[q]
ili kusanyiko lote la wana wa Israeli lipate kumsikiliza yeye.[r] **21** Naye atasimama mbele ya
Eleazari kuhani, naye atauliza[s] kwa ajili yake kulingana na hukumu ya Urimu[t] mbele za Yehova. Kwa agizo lake watatoka
nje na kwa agizo lake wataingia ndani, yeye na wana wote wa Israeli pamoja naye na kusanyiko lote."

22 Naye Musa akafanya
kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru. Kwa hiyo aka-

mchukua Yoshua na kumsimamisha mbele ya Eleazari[a] kuhani na mbele ya kusanyiko lote **23** na kuweka mikono yake juu yake na kumpa utume,[b] kama vile Yehova alivyokuwa amesema kupitia Musa.[c]

28 Na Yehova akazidi kusema na Musa, na kumwambia: **2** "Waamuru wana wa Israeli, nawe utawaambia, 'Muwe waangalifu na kunitolea toleo langu, mkate wangu,[d] kwa ajili ya matoleo yangu yanayotolewa kwa njia ya moto yakiwa harufu ya kunituliza,[e] kwenye nyakati zake zilizowekwa.'[f]

3 "Nawe utawaambia, 'Hili ndilo toleo linalotolewa kwa njia ya moto ambalo mtamtolea Yehova: wana-kondoo dume ambao hawana kasoro wenye umri wa mwaka mmoja, wawili kila siku wakiwa toleo la kuteketezwa daima.[g] **4** Mwana-kondoo dume mmoja utamtoa asubuhi, na yule mwana-kondoo dume mwingine utamtoa katikati ya zile jioni mbili,[h] **5** pamoja na sehemu ya kumi ya efa[i] ya unga laini ukiwa toleo la nafaka[j] lililotiwa sehemu ya nne ya hini ya mafuta yaliyopondwa;[k] **6** lile toleo la kuteketezwa la daima,[l] lililotolewa kwenye Mlima Sinai likiwa harufu ya kutuliza, toleo lililotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto,[m] **7** pamoja na toleo lake la kinywaji,[n] sehemu ya nne ya hini kwa kila mwana-kondoo dume.[o] Mimina katika mahali patakatifu lile toleo la kinywaji la kileo[p] kwa Yehova. **8** Nawe utamtoa yule mwana-kondoo dume mwingine katikati ya zile jioni mbili. Pamoja na toleo lilelile la nafaka kama lile la asubuhi na pamoja na toleo lake lilelile la kinywaji utalitoa likiwa toleo linalotolewa kwa njia ya moto, toleo lenye harufu ya kumtuliza Yehova.[a]

9 "'Hata hivyo, siku ya sabato[b] kutakuwa wana-kondoo dume wawili ambao hawana kasoro wenye umri wa mwaka mmoja na vipimo viwili vya sehemu ya kumi ya unga laini ukiwa toleo la nafaka lililotiwa mafuta, pamoja na toleo lake la kinywaji, **10** likiwa toleo la kuteketezwa la sabato katika sabato yake, pamoja na lile toleo la kuteketezwa la daima[c] na toleo lake la kinywaji.[d]

11 "'Na mwanzoni mwa miezi yenu mtamtolea Yehova toleo la kuteketezwa la ng'ombe-dume wawili wachanga na kondoo-dume mmoja, wana-kondoo dume saba ambao hawana kasoro kila mmoja akiwa na umri wa mwaka mmoja,[e] **12** na vipimo vitatu vya sehemu ya kumi ya unga laini ukiwa toleo la nafaka[f] lililotiwa mafuta kwa ajili ya kila ng'ombe-dume na vipimo viwili vya sehemu ya kumi ya unga laini ukiwa toleo la nafaka lililotiwa mafuta kwa ajili ya kondoo-dume mmoja,[g] **13** na kipimo kimoja cha sehemu ya kumi ya unga laini ukiwa toleo la nafaka lililotiwa mafuta kwa ajili ya kila mwana-kondoo dume, likiwa toleo la kuteketezwa, harufu ya kutuliza,[h] toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto. **14** Na kama matoleo yao ya kinywaji watatoa nusu[i] ya hini ya divai kwa ajili ya ng'ombe-dume na sehemu ya tatu[j] ya hini kwa ajili ya kondoo-dume na sehemu ya nne[k] ya hini kwa ajili ya mwana-kondoo dume.

SURA 27
a Hes 20:28
b Hes 27:18
Kum 31:14
c Kum 3:28
Kum 31:23

SURA 28
d Law 3:11
Law 21:6
Hes 28:24
Mal 1:7
e Mwa 8:21
Kut 29:18
Efe 5:2
Flp 4:18
f Kut 23:14
2Nya 8:13
Ezr 3:5
Ne 10:33
g Kut 29:38
Law 6:9
Hes 29:11
Eze 46:15
h Kut 12:6
Kut 29:39
Kum 16:6
i Kut 16:36
j Hes 15:4
k Kut 29:40
l Kut 29:42
2Nya 2:4
Ezr 3:3
m Law 8:21
n Law 23:13
o Kut 29:40
p Hes 15:10
Hes 28:14
Kum 14:26

Safu ya 2
a Kut 29:41
b Kut 16:29
Kut 20:10
Eze 20:12
c Hes 28:3
d Hes 28:7
e Hes 10:10
1Nya 23:31
2Nya 2:4
Ne 10:33
Kol 2:16
f Law 2:11
g Law 1:10
h Law 1:13
i Hes 15:10
j Hes 15:7
k Hes 15:5

Hilo ndilo toleo la kuteketezwa la kila mwezi katika mwezi wake kwa ajili ya miezi ya mwaka.[a] **15** Pia, mwana-mbuzi[b] mmoja atatolewa akiwa toleo la dhambi kwa Yehova kwa kuongezea lile toleo la kuteketezwa la daima pamoja na toleo lake la kinywaji.[c]

16 "'Na katika mwezi wa kwanza, siku ya kumi na nne ya mwezi huo, itakuwa pasaka ya Yehova.[d] **17** Na siku ya kumi na tano ya mwezi huu itakuwa sherehe. Keki zisizo na chachu zitaliwa kwa siku saba.[e] **18** Katika siku ya kwanza kutakuwako mkusanyiko mtakatifu.[f] Hamtafanya kazi ngumu ya aina yoyote.[g] **19** Nanyi mtatoa toleo linalotolewa kwa njia ya moto, toleo la kuteketezwa[h] kwa Yehova, ng'ombe-dume wawili wachanga na kondoo-dume mmoja na wana-kondoo dume saba kila mmoja akiwa na umri wa mwaka mmoja.[i] Wanapaswa kuwa wasio na kasoro kwa ajili yenu.[j] **20** Na kama matoleo yao ya nafaka[k] ya unga laini uliotiwa mafuta mtatoa vipimo vitatu vya sehemu ya kumi kwa ajili ya ng'ombe-dume na vipimo viwili vya sehemu ya kumi[l] kwa ajili ya kondoo-dume. **21** Utatoa kipimo kimoja cha sehemu ya kumi[m] kwa ajili ya kila mwana-kondoo dume kati ya wale wana-kondoo dume saba; **22** na mbuzi mmoja wa toleo la dhambi ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu.[n] **23** Mbali na lile toleo la kuteketezwa la asubuhi, ambalo ni kwa ajili ya toleo la kuteketezwa[o] la daima,[p] mtayatoa hayo. **24** Mtatoa matoleo kama hayo kila siku kwa zile siku saba kuwa mkate,[a] toleo linalotolewa kwa Yehova kwa njia ya moto,[b] lenye harufu ya kumtuliza Yehova. Litatolewa pamoja na toleo la kuteketezwa la daima, na toleo lake la kinywaji. **25** Na siku ya saba mtafanya mkusanyiko mtakatifu.[c] Hamtafanya kazi ngumu ya aina yoyote.[d]

26 "'Na katika siku ya matunda yaliyoiva ya kwanza,[e] mtakapomtolea Yehova toleo la nafaka mpya, katika sherehe yenu ya majuma[f] mtafanya mkusanyiko mtakatifu. Hamtafanya kazi ngumu ya aina yoyote.[g] **27** Nanyi mtatoa toleo la kuteketezwa kwa ajili ya harufu ya kumtuliza Yehova, ng'ombe-dume wawili wachanga, kondoo-dume mmoja, wana-kondoo dume saba kila mmoja akiwa na umri wa mwaka mmoja;[h] **28** na kama toleo lao la nafaka la unga laini uliotiwa mafuta, vipimo vitatu vya sehemu ya kumi kwa ajili ya kila ng'ombe-dume, vipimo viwili vya sehemu ya kumi[i] kwa ajili ya yule kondoo-dume, **29** kipimo kimoja cha sehemu ya kumi[j] vivyo hivyo kwa ajili ya kila mwana-kondoo dume kati ya wale wana-kondoo dume saba; **30** mwana-mbuzi mmoja ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu.[k] **31** Mbali na lile toleo la kuteketezwa la daima pamoja na toleo lake la nafaka mtawatoa.[l] Watakuwa wasio na kasoro kwenu,[m] pamoja na matoleo yao ya kinywaji.[n]

29 "'Na katika mwezi wa saba, siku ya kwanza ya mwezi huo, mtafanya mkusanyiko mtakatifu.[o] Hamtafanya kazi ngumu ya aina yoyote.[p] Itakuwa siku ya kupiga ta-

SURA 28
a Hes 29:6
b Law 4:23
Hes 15:24
Hes 28:22
c Hes 29:19
d Kut 12:14
Law 23:5
Kum 16:1
Eze 45:21
Lu 22:7
1Ko 5:7
e Kut 12:15
Law 23:6
1Ko 5:8
f Law 23:2
g Law 23:7
h Law 1:9
i Hes 28:11
j Law 22:20
Law 22:22
Kum 15:21
k Law 2:1
l Hes 28:12
m Hes 28:13
n Hes 28:15
Hes 29:5
o Hes 28:6
p Hes 28:3
Da 8:11
Da 11:31
Da 12:11

Safu ya 2
a Law 3:11
Law 21:6
Hes 28:2
b Hes 28:8
c Kut 12:16
Kut 13:6
Law 23:8
d Kum 16:8
e Kut 23:16
f Kut 34:22
Law 23:16
Law 23:21
Kum 16:10
Mdo 2:1
g Kut 31:14
Hes 28:18
h Law 23:18
i Hes 28:12
j Hes 28:13
k Law 23:19
Hes 28:15
l Hes 28:3
Hes 28:5
Hes 28:23
m Law 1:3
Hes 28:19
n Hes 28:7

SURA 29
o Law 23:24
p Law 23:25

rumbeta kwenu.[a] **2** Nanyi
mtatoa toleo la kuteketezwa
kuwa harufu ya kumtuliza Ye-
hova, ng'ombe-dume mmoja
mchanga, kondoo-dume mmo-
ja, wana-kondoo dume saba,
kila mmoja akiwa na umri wa
mwaka mmoja, ambao hawa-
na kasoro;[b] **3** na toleo lao
la nafaka la unga laini uliotiwa
mafuta, vipimo vitatu vya sehe-
mu ya kumi kwa ajili ya yule
ng'ombe-dume, vipimo viwili
vya sehemu ya kumi kwa aji-
li ya yule kondoo-dume,[c] **4** na
kipimo kimoja cha sehemu ya
kumi kwa ajili ya kila mmoja
kati ya wale wana-kondoo
saba;[d] **5** na mwana-mbuzi
mmoja akiwa toleo la dhambi
ili kufanya upatanisho kwa ajili
yenu;[e] **6** mbali na lile toleo la
kuteketezwa[f] la kila mwezi na
toleo lake la nafaka[g] na lile to-
leo la kuteketezwa la daima[h] na
toleo lake la nafaka,[i] pamoja na
matoleo yake ya kinywaji,[j] ku-
lingana na utaratibu wa kawai-
da kwa ajili yake, kuwa harufu
ya kutuliza, toleo linalotolewa
kwa Yehova kwa njia ya moto.[k]

7 "'Na katika siku ya kumi
ya mwezi huu mtafanya mkusa-
nyiko mtakatifu,[l] nanyi mtazi-
tesa nafsi zenu.[m] Hampaswi ku-
fanya kazi yoyote.[n] **8** Nanyi
mtamtolea Yehova toleo la ku-
teketezwa, lenye harufu ya ku-
tuliza, ng'ombe-dume mmoja
mchanga, kondoo-dume mmo-
ja, wana-kondoo dume saba
kila mmoja akiwa na umri wa
mwaka mmoja.[o] Watakuwa wa-
sio na kasoro kwa ajili yenu.[p]
9 Na likiwa toleo lao la nafa-
ka la unga laini uliotiwa mafu-
ta vipimo vitatu vya sehemu
ya kumi kwa ajili ya yule ng'o-
mbe-dume, vipimo viwili vya se-

SURA 29

a Hes 10:2
Zb 81:3
b Hes 28:19
c Hes 28:20
d Hes 28:21
e Hes 28:15
Hes 28:22
f Hes 28:11
g Hes 28:12
h Hes 28:3
i Hes 28:5
j Hes 28:7
k Law 23:25
Hes 28:6
l Law 16:29
Law 23:27
m Law 16:29
Law 23:29
Zb 35:13
Isa 58:5
n Law 23:31
o Hes 29:2
p Law 1:3
Law 22:22
Kum 15:21
Kum 17:1

Safu ya 2

a Hes 28:12
Hes 29:3
b Hes 28:13
Hes 29:4
c Law 16:3
d Hes 28:7
e Kut 23:16
Law 23:34
Kum 16:13
Ne 8:14
f Law 23:37
Ne 8:18
g Law 23:35
h Kum 16:15
i Law 1:3
Ezr 3:4
j Law 22:22
Kum 17:1
k Hes 28:12
Hes 29:3
l Hes 28:13
Hes 29:4
m Hes 28:3
Hes 28:5
Hes 28:7

hemu ya kumi kwa ajili ya yule
kondoo-dume mmoja,[a] **10** ki-
pimo kimoja cha sehemu ya
kumi vivyo hivyo kwa ajili ya
kila mmoja wa wale wana-ko-
ndoo saba;[b] **11** mwana-mbuzi
mmoja akiwa toleo la dhambi,
mbali na lile toleo la dhambi la
upatanisho[c] na lile toleo la ku-
teketezwa la daima na toleo
lake la nafaka, pamoja na mato-
leo yake ya kinywaji.[d]

12 "'Na katika siku ya kumi
na tano ya mwezi wa saba[e]
mtafanya mkusanyiko mtaka-
tifu.[f] Hamtafanya kazi ngumu
ya aina yoyote,[g] nanyi mtamfa-
nyia Yehova sherehe kwa siku
saba.[h] **13** Nanyi mtatoa to-
leo la kuteketezwa,[i] toleo lina-
lotolewa kwa njia ya moto, le-
nye harufu ya kumtuliza Ye-
hova, ng'ombe-dume wachanga
kumi na watatu, kondoo-dume
wawili, wana-kondoo dume
kumi na wanne kila mmoja wao
akiwa na umri wa mwaka mmo-
ja. Watakuwa wasio na kaso-
ro.[j] **14** Na toleo lao la nafa-
ka la unga laini uliotiwa mafu-
ta vipimo vitatu vya sehemu ya
kumi kwa ajili ya kila ng'ombe-
dume kati ya wale ng'ombe-
dume kumi na watatu, vipi-
mo viwili vya sehemu ya kumi
kwa ajili ya kila kondoo-dume
kati ya wale kondo-dume wawi-
li,[k] **15** na kipimo kimoja cha
sehemu ya kumi kwa ajili ya
kila mwana-kondoo dume kati
ya wale wana-kondoo kumi na
wanne;[l] **16** na mwana-mbuzi
mmoja akiwa toleo la dhambi,
mbali na lile toleo la kuketete-
zwa la daima, toleo lake la nafa-
ka na toleo lake la kinywaji.[m]

17 "'Na katika siku ya pili
ng'ombe-dume wachanga kumi
na wawili, kondoo-dume wawili,

wana-kondoo dume kumi na
wanne kila mmoja akiwa na
umri wa mwaka mmoja, ambao
hawana kasoro;[a] **18** na toleo
lao la nafaka[b] na matoleo yao ya
kinywaji[c] kwa ajili ya wale ng'o-
mbe-dume, wale kondoo-dume
na wale wana-kondoo kwa he-
sabu yao kulingana na utarati-
bu wa kawaida;[d] **19** na mwa-
na-mbuzi mmoja akiwa toleo la
dhambi,[e] mbali na lile toleo la
kuketetezwa la daima na toleo
lake la nafaka, pamoja na mato-
leo yake ya kinywaji.[f]

20 "'Na katika siku ya tatu
ng'ombe-dume kumi na mmo-
ja, kondoo-dume wawili, wana-
kondoo dume kumi na wanne
kila mmoja wao akiwa na umri
wa mwaka mmoja, ambao ha-
wana kasoro;[g] **21** na toleo lao
la nafaka[h] na matoleo yao ya ki-
nywaji[i] kwa ajili ya wale ng'o-
mbe-dume, wale kondoo-dume
na wale wana-kondoo kwa he-
sabu yao kulingana na utarati-
bu wa kawaida; **22** na mbuzi
mmoja akiwa toleo la dhambi,[j]
mbali na lile toleo la kuketete-
zwa la daima na toleo lake la na-
faka na toleo lake la kinywaji.

23 "'Na katika siku ya nne
ng'ombe-dume kumi, kondoo-
dume wawili, wana-kondoo
dume kumi na wanne kila mmo-
ja wao akiwa na umri wa mwa-
ka mmoja, ambao hawana ka-
soro;[k] **24** toleo lao la nafaka[l]
na matoleo yao ya kinywaji[m]
kwa ajili ya wale ng'ombe-
dume, wale kondoo-dume na
wale wana-kondoo kwa hesabu
yao kulingana na utaratibu wa
kawaida;[n] **25** na mwana-mbu-
zi mmoja akiwa toleo la dha-
mbi,[o] mbali na lile toleo la kute-
ketezwa[p] la daima na toleo lake
la nafaka na toleo lake la ki-
nywaji.[q]

SURA 29

a Kum 15:21
b Hes 29:3
Hes 29:14
c Hes 28:14
d Hes 28:12
e Hes 28:15
f Hes 28:3
Hes 28:5
Hes 28:7
g Hes 29:13
h Hes 29:9
Hes 29:14
i Hes 28:14
j Hes 28:15
k Law 22:22
Hes 29:13
l Hes 29:14
m Hes 28:14
n Hes 28:12
o Law 4:23
Hes 28:15
p Hes 28:3
q Hes 28:7

Safu ya 2

a Kum 15:21
Kum 17:1
b Hes 29:14
c Hes 28:14
d Hes 28:12
e Law 4:23
Hes 28:15
f Hes 28:7
g Law 1:3
Hes 29:8
h Hes 29:3
Hes 29:14
i Hes 28:14
j Hes 28:12
k Law 4:23
Hes 28:15
l Hes 28:7
m Law 1:3
Law 22:22
n Hes 29:3
Hes 29:14
o Hes 28:14
p Hes 28:12
q Law 4:23
Hes 28:15

26 "'Na katika siku ya
tano ng'ombe-dume tisa, kon-
doo-dume wawili, wana-kon-
doo dume kumi na wanne kila
mmoja wao akiwa na umri wa
mwaka mmoja, ambao hawa-
na kasoro;[a] **27** na toleo lao
la nafaka[b] na matoleo yao ya ki-
nywaji[c] kwa ajili ya wale ng'o-
mbe-dume, wale kondoo-dume
na wale wana-kondoo kwa he-
sabu yao kulingana na utarati-
bu wa kawaida;[d] **28** na mbuzi
mmoja akiwa toleo la dhambi,[e]
mbali na lile toleo la kuketete-
zwa la daima na toleo lake la na-
faka na toleo lake la kinywaji.[f]

29 "'Na katika siku ya sita
ng'ombe-dume wanane, kon-
doo-dume wawili, wana-kon-
doo dume kumi na wanne kila
mmoja wao akiwa na umri wa
mwaka mmoja, ambao hawa-
na kasoro;[g] **30** na toleo lao
la nafaka[h] na matoleo yao ya ki-
nywaji[i] kwa ajili ya wale ng'o-
mbe-dume, wale kondoo-dume
na wale wana-kondoo kwa he-
sabu yao kulingana na utarati-
bu wa kawaida;[j] **31** na mbuzi
mmoja akiwa toleo la dhambi,[k]
mbali na lile toleo la kuketete-
zwa la daima na toleo lake la
nafaka na matoleo yake ya ki-
nywaji.[l]

32 "'Na katika siku ya
saba ng'ombe-dume saba, kon-
doo-dume wawili, wana-kon-
doo dume kumi na wanne kila
mmoja wao akiwa na umri wa
mwaka mmoja, ambao hawa-
na kasoro;[m] **33** na toleo lao
la nafaka[n] na matoleo yao ya ki-
nywaji[o] kwa ajili ya wale ng'o-
mbe-dume, wale kondoo-dume
na wale wana-kondoo kwa he-
sabu yao kulingana na utarati-
bu wa kawaida;[p] **34** na mbuzi
mmoja akiwa toleo la dhambi,[q]

mbali na lile toleo la kuteketezwa la daima na toleo lake la nafaka na toleo lake la kinywaji.[a]

35 "'Na katika siku ya nane mtafanya kusanyiko kuu.[b] Hamtafanya kazi ngumu ya aina yoyote.[c] **36** Nanyi mtatoa toleo la kuteketezwa, toleo linalotolewa kwa njia ya moto, lenye harufu ya kumtuliza Yehova, ng'ombe-dume mmoja, kondoo-dume mmoja, wana-kondoo dume saba kila mmoja wao akiwa na umri wa mwaka mmoja, ambao hawana kasoro;[d] **37** na toleo lao la nafaka[e] na matoleo yao ya kinywaji[f] kwa ajili ya yule ng'ombe-dume, yule kondoo-dume na wale wana-kondoo kwa hesabu yao kulingana na utaratibu wa kawaida;[g] **38** na mbuzi mmoja akiwa toleo la dhambi,[h] mbali na lile toleo la kuteketezwa la daima na toleo lake la nafaka na toleo lake la kinywaji.[i]

39 "'Hayo mtamtolea Yehova kwenye sherehe zenu za majira,[j] mbali na matoleo yenu ya nadhiri[k] na matoleo yenu ya hiari[l] yakiwa matoleo yenu ya kuteketezwa[m] na matoleo yenu ya nafaka[n] na matoleo yenu ya kinywaji[o] na dhabihu zenu za ushirika.'"[p] **40** Naye Musa akaongea na wana wa Israeli kulingana na kila jambo ambalo Yehova alikuwa amemwamuru Musa.[q]

30 Ndipo Musa akasema na vichwa[r] vya makabila ya wana wa Israeli, na kuwaambia: "Hili ndilo neno ambalo Yehova ameamuru: **2** Ikiwa mwanamume ataweka nadhiri[s] kwa Yehova au ikiwa ataapa kiapo[t] ili kufunga nadhiri ya kujiepusha[u] juu ya nafsi yake, hapaswi kulivunja neno lake.[v] Anapaswa kufanya kulingana na yote ambayo yametoka kinywani mwake.[a]

3 "Na ikiwa mwanamke ataweka nadhiri kwa Yehova[b] au akijifunga kwa nadhiri ya kujiepusha katika nyumba ya baba yake wakati wa ujana wake, **4** na kwa kweli baba yake asikie nadhiri yake au nadhiri yake ya kujiepusha ambayo amefunga juu ya nafsi yake, na baba yake akae kimya kumwelekea, nadhiri zake zote zitasimama pia, na kila nadhiri ya kujiepusha[c] ambayo amefunga juu ya nafsi yake itasimama. **5** Lakini ikiwa baba yake amemkataza katika siku ya kusikia kwake nadhiri zake zote au nadhiri zake za kujiepusha ambazo amefunga juu ya nafsi yake, haitasimama, bali Yehova atamsamehe, kwa sababu baba yake alimkataza.[d]

6 "Hata hivyo, ikiwa yeye ana mume, nayo nadhiri yake iko juu yake[e] au ile ahadi ya midomo yake, iliyotolewa bila kufikiri, iko juu ya nafsi yake, **7** na kwa kweli mume wake asikie na kukaa kimya kumwelekea siku ya kusikia kwake, nadhiri zake zitasimama au nadhiri zake za kujiepusha ambazo amefunga juu ya nafsi yake zitasimama.[f] **8** Lakini ikiwa mume wake atamkataza katika siku ya kusikia kwake,[g] yeye pia ameifuta nadhiri yake iliyokuwa juu yake au ile ahadi ya midomo yake, iliyotolewa bila kufikiri, ambayo aliifunga juu ya nafsi yake, na Yehova atamsamehe.[h]

9 "Kuhusu nadhiri ya mjane au mwanamke aliyepewa talaka, kila jambo ambalo amefunga juu ya nafsi yake litasimama dhidi yake.

SURA 29
a Hes 28:7
b Law 23:36
c Law 23:39
d Hes 29:2
e Hes 29:3
Hes 29:14
f Hes 28:14
g Hes 28:12
h Law 4:23
Hes 28:15
i Hes 28:7
j Law 23:2
Kum 16:16
k Hes 15:3
Kum 12:6
l Law 7:16
Law 22:21
m Law 1:3
n Law 2:1
o Hes 15:5
p Law 3:1
q Kut 40:16
Kum 4:5

SURA 30
r Kut 18:25
s Mwa 28:20
Law 27:2
Amu 11:30
t Hes 30:10
Zb 132:2
u Hes 30:11
Mdo 23:14
v Kum 23:21
Zb 76:11
Zb 116:14
Zb 119:106
Mhu 5:4
Mt 5:33

Safu ya 2
a Zb 22:25
Zb 50:14
Zb 66:13
Nah 1:15
b 1Sa 1:11
c Hes 30:10
Hes 30:13
d Mk 7:10
Efe 6:1
e 1Sa 1:11
1Sa 1:22
f 1Sa 1:23
g Ro 7:2
1Ko 11:3
Efe 5:22
h Hes 30:5

10 "Hata hivyo, ikiwa ameweka nadhiri au amefunga nadhiri ya kujiepusha juu ya nafsi yake kwa kiapo[a] katika nyumba ya mume wake, **11** na mume wake awe amesikia jambo hilo na kukaa kimya kumwelekea, hakumkataza; na nadhiri zake zote zitasimama au nadhiri yoyote ya kujiepusha ambayo amefunga juu ya nafsi yake itasimama. **12** Lakini ikiwa mume wake amezifuta kabisa katika siku ya kusikia kwake maneno yoyote ya midomo yake yakiwa nadhiri zake au nadhiri ya kujiepusha ya nafsi yake, hazitasimama.[b] Mume wake amezifuta, na Yehova atamsamehe.[c] **13** Nadhiri yoyote au kiapo chochote cha kujiepusha ili kuitesa nafsi,[d] mume wake atakiimarisha au mume wake atakifuta. **14** Lakini ikiwa mume wake atakaa kimya kabisa kumwelekea siku baada ya siku, yeye ameziimarisha pia nadhiri zake zote au nadhiri zake zote za kujiepusha zilizo juu yake.[e] Amezithibitisha kwa sababu alikaa kimya kumwelekea siku alipozisikia. **15** Na ikiwa atazifuta kabisa baada ya yeye kuzisikia, kwa kweli pia analichukua kosa la mke wake.[f]

16 "Hayo ndiyo masharti ambayo Yehova alimwamuru Musa yawe kati ya mume na mke wake,[g] kati ya baba na binti yake wakati wa ujana wake katika nyumba ya baba yake."[h]

31 Kisha Yehova akasema na Musa, na kumwambia: **2** "Lipiza kisasi[i] kwa ajili ya wana wa Israeli juu ya Wamidiani.[j] Baadaye utakusanywa kwa watu wako."[k]

3 Basi Musa akasema na watu, na kuwaambia: "Tayarisheni wanaume kati yenu kwa ajili ya jeshi, watumiwe kupiga Midiani ili kulipiza kisasi cha Yehova juu ya Midiani.[a] **4** Watu elfu moja wa kila kabila kati ya makabila yote ya Israeli mtawatuma katika jeshi." **5** Kwa hiyo kutoka kati ya maelfu[b] ya Israeli watu elfu moja katika kabila walipewa mgawo, kumi na mbili elfu waliotayarishwa kwa ajili ya jeshi.[c]

6 Ndipo Musa akawatuma, watu elfu moja wa kila kabila, kwenye jeshi, wao na Finehasi[d] mwana wa Eleazari kuhani kwenye jeshi, na vile vyombo vitakatifu na zile tarumbeta[e] za kupiga mbiu zilikuwa mkononi mwake. **7** Nao wakapigana vita na Midiani, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa, nao wakamuua kila mwanamume.[f] **8** Nao wakawaua wafalme wa Midiani pamoja na wengine waliouawa, yaani, Evi na Rekemu na Suri na Huru na Reba, wale wafalme watano wa Midiani;[g] nao wakamuua Balaamu[h] mwana wa Beori kwa upanga. **9** Lakini wana wa Israeli wakawachukua mateka wanawake wa Midiani na watoto wao wadogo;[i] na wanyama wao wote wa kufugwa na mifugo yao yote na riziki yao yote wakaipora. **10** Nayo majiji yao yote walimokuwa wamefanya makao na kambi zao zenye kuta wakaziteketeza kwa moto.[j] **11** Nao wakachukua nyara[k] zote na kuteka nyara binadamu na wanyama wote wa kufugwa. **12** Nao wakamletea Musa na Eleazari kuhani na kusanyiko la wana wa Israeli mateka na nyara na vitu vilivyoporwa, mpaka kambini, mpaka nchi tambarare

SURA 30
a Hes 30:6
b 1Ko 11:3; 1Pe 3:1
c Hes 30:5; Hes 30:8
d Zb 35:13; Isa 58:5
e Hes 30:7
f Kum 23:21
g Hes 30:6; Hes 30:10
h Hes 30:3

SURA 31
i Kum 32:41; Zb 94:1; Isa 1:24; Nah 1:2
j Hes 25:2; Hes 25:17
k Hes 27:13; Kum 32:50

Safu ya 2
a Hes 22:7; Hes 25:18; 1Ko 10:8; Ufu 2:14
b Hes 26:51
c Law 26:8
d Hes 25:7; Hes 25:11
e Hes 10:2; Hes 10:9
f Kum 20:13
g Yos 13:21
h Hes 22:12; Hes 24:25; Yos 13:22; 2Pe 2:15; Yud 11; Ufu 2:14
i Kum 20:14
j Yos 6:24
k Kum 2:35; Yos 8:2

za jangwa la Moabu,[a] kando ya
Yordani huko Yeriko.
13 Ndipo Musa na Eleazari
kuhani na wakuu wote wa ku-
sanyiko wakatoka nje ili wa-
kutane nao nje ya kambi.
14 Na Musa akaanza kuwa na
ghadhabu kwa sababu ya wale
wanaume waliowekwa rasmi
wa majeshi ya vita,[b] wakuu
wa maelfu na wakuu wa ma-
mia waliokuwa wakiingia ku-
toka katika safari hiyo ya ki-
jeshi. **15** Kwa hiyo Musa aka-
waambia: "Je, mmemhifadhi
hai kila mwanamke?[c] **16** Ta-
zama! Hao ndio, kupitia kwa
neno la Balaamu, waliowasha-
wishi wana wa Israeli kuko-
sa uaminifu[d] kwa Yehova juu ya
lile jambo la Peori,[e] hivi kwa-
mba tauni ikaja juu ya kusanyi-
ko la Yehova.[f] **17** Na sasa ueni
kila mtoto wa kiume, na ku-
muua kila mwanamke ambaye
amefanya ngono na mtu
kwa kulala na mwanamume.[g]
18 Na mwahifadhi hai kwa aji-
li yenu watoto wote kati ya wa-
nawake ambao hawajajua te-
ndo la kulala na mwanamu-
me.[h] **19** Nanyi mpige kambi
nje ya kambi siku saba. Kila
mtu ambaye ameua nafsi[i] na
kila mtu ambaye amegusa mtu
aliyeuawa,[j] mtajitakasa[k] kati-
ka siku ya tatu na katika siku
ya saba, ninyi na mateka wenu.
20 Na kila vazi na kila cho-
mbo cha ngozi na kila kitu ki-
lichotengenezwa kwa manyoya
ya mbuzi na kila chombo cha
mbao mtajitakasia kutoka kati-
ka dhambi."[l]
21 Ndipo Eleazari kuhani
akawaambia wanaume wa jeshi
waliokuwa wameenda kwenye
pigano: "Hii ndiyo amri ya she-
ria ambayo Yehova amemwa-
muru Musa, **22** 'Ni dhahabu
na fedha, shaba, chuma, bati na
risasi tu, **23** kila kitu amba-
cho hustahimili moto, ndicho
mtakachokipitisha motoni,[a] na-
cho kitakuwa safi. Ila kina-
paswa kutakaswa kwa kutu-
mia maji ya kutakasa.[b] Na kila
kitu ambacho hakiwezi ku-
stahimili moto mtakipitisha
katika maji.[c] **24** Nanyi mta-
yafua mavazi yenu katika siku
ya saba na kuwa safi, na baa-
daye mtaweza kuingia ndani ya
kambi.'"[d]
25 Na Yehova akamwambia
Musa hivi: **26** "Chukua hesa-
bu ya nyara, mateka ya binada-
mu na pia ya wanyama wa kufu-
gwa, wewe na Eleazari kuhani
na vichwa vya baba za kusanyi-
ko. **27** Nawe utagawa nyara
katika sehemu mbili kati ya
wale walioshiriki katika pigano
ambao walitoka nje kufunga sa-
fari na wale wengine wote wa
kusanyiko.[e] **28** Nawe utachu-
kua iwe kodi[f] kwa ajili ya Ye-
hova kutoka kwa wanaume wa
vita waliotoka nje kwenda safa-
rini nafsi moja kati ya mia
tano, ya binadamu na ya mi-
fugo na ya punda na ya ku-
ndi. **29** Kutoka katika nusu
yao utachukua na kumpa Elea-
zari kuhani wawe mchango wa
Yehova.[g] **30** Na kutoka kati-
ka nusu ya wana wa Israeli uta-
chukua mmoja kati ya 50, kati
ya binadamu, kati ya mifugo,
kati ya punda na kati ya kundi,
kati ya kila namna ya wanya-
ma wa kufugwa, nawe utawa-
pa Walawi,[h] watunzaji wa waji-
bu wa maskani ya Yehova."[i]
31 Na Musa na Eleazari ku-
hani wakafanya kama vile Ye-
hova alivyokuwa amemwamuru
Musa. **32** Na nyara, mabaki
ya vitu vilivyoporwa ambavyo

SURA 31
a Hes 22:1
b Hes 31:5
c Yer 48:10
d Hes 25:2
2Pe 2:15
Ufu 2:14
e Hes 25:18
Kum 4:3
Yos 22:17
f Hes 25:9
1Ko 10:8
g Amu 21:11
h Hes 31:35
i Hes 5:2
Hes 19:11
j Hes 19:16
k Hes 19:20
l Hes 31:23

Safu ya 2
a Met 17:3
Met 25:4
b Hes 19:9
c Hes 31:20
d Hes 19:19
Hes 19:20
e Yos 22:8
1Sa 30:24
Zb 68:12
f Mwa 14:20
1Nya 26:27
g Hes 18:20
Hes 18:29
h Kum 12:12
Kum 12:19
Yos 13:14
i Hes 3:7
Hes 18:3
1Nya 23:32

watu wa ile safari walikuwa
wamechukua vikiwa nyara, zi-
kajumlika kuwa kundi la wa-
nyama 675,000, **33** na mifugo
72,000, **34** na punda 61,000.
35 Nazo nafsi[a] za binadamu ku-
toka kati ya wanawake ambao
hawakuwa wamejua tendo la
kulala na mwanamume,[b] nafsi
zote zilikuwa 32,000. **36** Na
ile nusu iliyokuwa fungu la
wale waliotoka kwenda safari-
ni hesabu yake ilijumlika
kuwa kundi la wanyama 337,-
500. **37** Nayo kodi[c] ya Yeho-
va kutoka katika kundi ikaju-
mlika kuwa 675. **38** Na kati
ya wanyama wa mifugo kuli-
kuwa na 36,000, nayo kodi juu
yao kwa ajili ya Yehova ilikuwa
72. **39** Nao punda walikuwa
30,500, nayo kodi juu yao
kwa ajili ya Yehova ilikuwa 61.
40 Nazo nafsi za binadamu zili-
kuwa 16,000, nayo kodi juu yao
kwa ajili ya Yehova ilikuwa
nafsi 32. **41** Ndipo Musa aka-
mpa Eleazari kuhani ile kodi
iwe mchango wa Yehova,[d] kama
vile Yehova alivyokuwa ame-
mwamuru Musa.[e]

42 Na kutoka katika ile nusu
ya wana wa Israeli, ambayo
Musa aligawa kutoka katika
ile mali ya wanaume waliopi-
ga vita: **43** Sasa nusu ya kusa-
nyiko kutoka katika kundi ilijum-
lika kuwa 337,500, **44** na ya
mifugo, 36,000 **45** na punda,
30,500, **46** na nafsi za bina-
damu, 16,000. **47** Kisha Musa
akachukua kutoka katika ile
nusu ya wana wa Israeli ile ya
kutolewa katika 50, ya binada-
mu na ya wanyama wa kufugwa,
na kuwapa Walawi,[f] watunzaji
wa wajibu[g] wa maskani ya Yeho-
va, kama vile Yehova alivyoku-
wa amemwamuru Musa.

SURA 31

a Mwa 2:7
1Ko 15:45
b Hes 31:18
c Mwa 14:20
1Nya 26:27
d Hes 18:8
Hes 18:19
1Ko 9:14
Ga 6:6
Ebr 7:5
e Hes 5:9
f Kum 12:12
Kum 12:19
g Hes 3:7
Hes 18:3
Hes 31:30
1Nya 23:32

Safu ya 2

a Hes 31:4
b Hes 1:4
Hes 1:16
Hes 31:14
Kum 1:15
c Kut 23:27
Law 26:7
d Zb 96:8
e Mwa 41:42
f Kut 35:22
g Hes 18:8
Hes 18:19
h Kum 20:14
i Kut 30:16

SURA 32

j Hes 26:7
Yos 13:15
k Hes 26:18
Yos 13:24
l Hes 21:32
Yos 13:25
Isa 16:8
m Hes 32:34
n Hes 21:30
Yos 13:9

48 Nao watu waliowekwa ra-
smi ambao walikuwa wa yale
maelfu ya jeshi,[a] wakuu wa ma-
elfu na wakuu wa mamia,[b] wa-
kamkaribia Musa, **49** na ku-
mwambia Musa: "Watumishi
wako wamechukua hesabu ya
wanaume wa vita walio chini
ya usimamizi wetu wala hakuna
hata mmoja aliyesemwa kuwa
anakosekana kwetu.[c] **50** Kwa
hiyo na tutoe kila mmoja kile
ambacho amepata kiwe toleo la
Yehova,[d] vyombo vya dhahabu,
mikufu ya mguuni, na vikuku,
pete za muhuri,[e] vipuli, na ma-
pambo ya kike,[f] ili kufanya upa-
tanisho kwa ajili ya nafsi zetu
mbele za Yehova."

51 Basi Musa na Eleazari
kuhani wakakubali dhahabu
hiyo kutoka kwao,[g] vito vyo-
te. **52** Nayo dhahabu yote ya
mchango ambayo walimchangia
Yehova ikajumlika kuwa sheke-
li 16,750, kutoka kwa wakuu wa
maelfu na wakuu wa mamia.
53 Wanaume wa jeshi walikuwa
wamepora vitu kila mmoja kwa
ajili yake mwenyewe.[h] **54** Basi
Musa na Eleazari kuhani wa-
kaikubali dhahabu hiyo kuto-
ka kwa wakuu wa maelfu na
kwa wakuu wa mamia na kui-
leta ndani ya hema la mkutano
iwe ukumbusho[i] kwa wana wa
Israeli mbele za Yehova.

32 Sasa wana wa Rubeni[j] na
wana wa Gadi[k] wakawa
na mifugo mingi, mingi sana,
kwa kweli. Nao wakaanza kuio-
na nchi ya Yazeri[l] na nchi ya Gi-
leadi, na, tazama! mahali hapo
palikuwa mahali pa mifugo.
2 Basi wana wa Gadi na wana
wa Rubeni wakaja na kumwa-
mbia Musa na Eleazari kuhani
na wakuu wa kusanyiko, jambo
hili: **3** "Atarothi[m] na Diboni[n]

na Yazeri na Nimra[a] na Heshboni[b] na Eleale[c] na Sebamu
na Nebo[d] na Beoni,[e] **4** nchi
ambayo Yehova alishinda[f] mbe-
le ya kusanyiko la Israeli, ni
nchi ya mifugo, nao watumishi
wako wana mifugo."[g] **5** Nao
wakaendelea kusema: "Ikiwa
tumepata kibali machoni pako,
acheni watumishi wako wape-
we nchi hiyo iwe miliki yao. Usi-
tufanye tuvuke Yordani."[h]

6 Basi Musa akawaambia
wana wa Gadi na wana wa Ru-
beni: "Je, ndugu zenu wataenda
vitani huku ninyi mkiendelea
kukaa hapa?[i] **7** Na kwa nini
mwavunje moyo wana wa Israe-
li wasivuke kuingia katika nchi
ambayo hakika Yehova atawa-
pa wao? **8** Hivyo ndivyo baba
zenu walivyofanya[j] nilipowatu-
ma kutoka Kadesh-barnea[k] wa-
kaione nchi. **9** Walipoenda
kwenye bonde la mto la Eshko-
li[l] na kuiona nchi, ndipo wali-
powavunja moyo wana wa Isra-
eli, ili wasiingie katika nchi
ambayo kwa hakika Yehova
angewapa.[m] **10** Basi hasira ya
Yehova ikawaka siku hiyo hivi
kwamba akaapa,[n] na kusema,
11 'Wanaume waliotoka Mi-
sri kuanzia umri wa miaka 20
na zaidi[o] hawatauona udongo
ambao niliwaapia Abrahamu,
Isaka na Yakobo,[p] kwa sababu
hawakunifuata kabisa, **12** isi-
pokuwa Kalebu[q] mwana wa Ye-
fune Mkenizi na Yoshua[r] mwa-
na wa Nuni, kwa sababu wame-
mfuata Yehova kikamilifu.'
13 Basi hasira ya Yehova ika-
waka juu ya Israeli naye aka-
wafanya watange-tange nyika-
ni miaka 40,[s] mpaka kizazi cho-
te kilichokuwa kikifanya uovu
machoni pa Yehova kikafikia
mwisho wake.[t] **14** Na tazama,

SURA 32

a Hes 32:36
b Hes 21:26
c Hes 32:37
Yer 48:34
d Hes 33:47
e Hes 32:38
f Hes 21:24
Kum 2:24
Kum 3:18
g Mwa 46:34
Kum 2:35
h Yos 1:12
Yos 1:14
Yos 13:8
i Flp 2:4
j Hes 13:31
Yos 14:8
k Yos 14:7
l Hes 13:23
Kum 1:24
m Hes 13:32
Kum 1:26
n Hes 14:28
Kum 1:34
Zb 95:11
Eze 20:15
Ebr 3:18
o Hes 14:29
Kum 1:35
Kum 2:14
p Mwa 13:15
Mwa 26:3
Mwa 28:13
q Hes 13:30
Hes 14:24
Kum 1:36
Yos 14:8
r Hes 14:30
Kum 1:38
Yos 19:49
s Hes 14:33
Kum 29:5
Yos 5:6
Zb 95:10
Mdo 7:36
Mdo 13:18
t Hes 26:64
Kum 2:14
1Ko 10:5
Ebr 3:17

Safu ya 2

a Kum 1:34
Mdo 7:51
b Ebr 10:38
c Kut 23:21
d 2Nya 15:2
e Kum 3:18
Yos 4:12
f Yos 22:4
g Hes 32:33
Yos 12:1
Yos 13:8
2Fa 10:33
h Kum 3:18
Yos 1:14
Yos 4:13
i Zb 78:55
j Kum 3:20
Yos 11:23
Yos 18:1
Zb 44:2
k Yos 22:4
Yos 22:9

ninyi mmesimama mahali pa
baba zenu kama kundi la watu
wenye dhambi ili kuizidisha ha-
sira ya Yehova[a] inayowaka juu
ya Israeli. **15** Ikiwa mtageu-
ka na kuacha kumfuata,[b] yeye
naye pia bila shaka atawaa-
cha wao tena wakae muda mre-
fu zaidi nyikani,[c] nanyi mtaku-
wa mmewatendea kwa uharibi-
fu watu hawa wote."[d]

16 Baadaye wakamkaribia
na kusema: "Acha tujenge hapa
mazizi ya mawe ya makundi
kwa ajili ya mifugo yetu na ma-
jiji kwa ajili ya watoto wetu wa-
dogo. **17** Lakini sisi wenyewe
tutaenda tayari tukiwa tume-
jipanga kivita[e] mbele ya wana
wa Israeli mpaka tutakapoku-
wa tumewafikisha mahali pao,
nao watoto wetu wadogo wa-
takaa katika majiji yenye ngo-
me mbali na uso wa wakaaji
wa nchi. **18** Hatutarudi kati-
ka nyumba zetu mpaka wana
wa Israeli watakapokuwa wa-
memiliki nchi, kila mmoja aki-
wa na urithi wake mwenyewe.[f]
19 Kwa maana hatutapata uri-
thi pamoja nao kuanzia upande
wa Yordani na ng'ambo, kwa sa-
babu urithi wetu umetujia upa-
nde wa Yordani kuelekea ma-
shariki."[g]

20 Basi Musa akawaambia:
"Ikiwa mtafanya hivyo, iki-
wa mtajitayarisha mbele za Ye-
hova kwa ajili ya vita,[h] **21** na
kila mmoja wenu aliye taya-
ri kwa kweli atavuka Yordani
mbele za Yehova, mpaka
atakapokuwa amewafukuzia
mbali adui zake kutoka mbe-
le zake,[i] **22** na nchi iwe ime-
tiishwa mbele za Yehova,[j] ki-
sha mrudi baadaye,[k] ninyi pia
mtajionyesha kuwa mko huru
na hatia juu ya Yehova na juu ya

Israeli; nayo nchi hii itakuwa
miliki yenu mbele za Yehova.[a]
23 Lakini ikiwa hamtafanya
hivyo, mtakuwa mmemtendea
Yehova dhambi.[b] Na kwa hiyo
jueni kwamba dhambi yenu ita-
wafikia ninyi.[c] **24** Jijengeeni
majiji kwa ajili ya watoto wenu
wadogo na mazizi ya mawe kwa
ajili ya makundi yenu, nanyi
mnapaswa kufanya jambo lililo-
toka kinywani mwenu."[d]

25 Ndipo wana wa Gadi na
wana wa Rubeni wakamwa-
mbia Musa hivi: "Watumi-
shi wako watafanya kama vile
bwana wangu anavyoamuru.[e]
26 Watoto wetu wadogo, wake
zetu, mifugo yetu na wanyama
wetu wote wa kufugwa wata-
kaa huko katika majiji ya Gilea-
di,[f] **27** lakini watumishi wako
watavuka, kila mtu aliye tayari
kwa ajili ya jeshi,[g] mbele za Ye-
hova kwa ajili ya vita, kama vile
bwana wangu anavyosema."

28 Basi Musa akatoa amri
juu yao kwa Eleazari kuha-
ni na Yoshua mwana wa Nuni
na vichwa vya upande wa baba
vya makabila ya wana wa Israe-
li. **29** Kwa hiyo Musa akawa-
ambia: "Ikiwa wana wa Gadi na
wana wa Rubeni watavuka pa-
moja nanyi Yordani, kila mtu
aliye tayari kwa ajili ya vita,[h]
mbele za Yehova, nayo nchi itii-
shwe mbele yenu, basi ninyi
mtawapa nchi ya Gileadi iwe
miliki yao.[i] **30** Lakini wasipo-
vuka wakiwa tayari pamoja na-
nyi, basi watapewa makao ka-
tikati yenu katika nchi ya Ka-
naani."[j]

31 Ndipo wana wa Gadi na
wana wa Rubeni wakajibu, na
kusema: "Jambo ambalo Ye-
hova amewaambia watumishi
wako ndivyo tutakavyofanya.[k]
32 Sisi wenyewe tutavuka tu-
kiwa tayari mbele za Yehova
mpaka nchi ya Kanaani,[a] na
miliki ya urithi wetu itaku-
wa pamoja nasi upande huu wa
Yordani."[b] **33** Basi Musa aka-
wapa, yaani, wana wa Gadi[c]
na wana wa Rubeni[d] na nusu
ya kabila la Manase[e] mwana wa
Yosefu, ufalme wa Sihoni[f] mfa-
lme wa Waamori na ufalme wa
Ogu[g] mfalme wa Bashani, nchi
ya majiji yake katika maeneo,
na majiji ya nchi kuzunguka
pande zote.

34 Na wana wa Gadi waka-
jenga Diboni[h] na Atarothi[i] na
Aroeri,[j] **35** na Atroth-shofani
na Yazeri[k] na Yogbeha,[l] **36** na
Beth-nimra[m] na Beth-harani,[n]
majiji yenye ngome,[o] na mazizi
ya mawe ya makundi.[p] **37** Na
wana wa Rubeni wakajenga He-
shboni[q] na Eleale[r] na Kiriathaim-
mu,[s] **38** na Nebo[t] na Baal-me-
oni[u]—majina yao yakiwa yame-
badilishwa—na Sibma; nao wa-
kaanza kuyaita kwa majina yao
wenyewe majiji waliyojenga.

39 Nao wana wa Makiri[v]
mwana wa Manase wakapiga
mwendo mpaka Gileadi, wakali-
teka, wakawafukuzia mbali Wa-
amori waliokuwamo. **40** Basi
Musa akampa Makiri mwana
wa Manase, Gileadi, naye aka-
kaa humo.[w] **41** Na Yairi mwa-
na wa Manase akapiga mwendo,
akateka vijiji vyao vya mahema,
naye akaanza kuviita Hawoth-
yairi.[x] **42** Naye Noba akapiga
mwendo, akaliteka Kenathi[y] na
miji yake ya kandokando; naye
akaanza kuliita Noba kwa jina
lake mwenyewe.

33 Hivi ndivyo vilivyoku-
wa vituo vya wana wa
Israeli waliotoka nchi ya Misri[z]
kwa majeshi[a] yao kwa mkono
wa Musa na Haruni.[b] **2** Naye

SURA 32
a Kum 3:12
Yos 1:15
Yos 13:8
b Hes 15:22
Yak 4:17
c Met 13:21
Isa 59:12
Ga 6:7
d Hes 32:16
Hes 32:34
Hes 32:37
e Yos 1:13
f Yos 1:14
g Yos 4:12
h Hes 32:20
i Yos 1:15
Yos 13:15
Yos 13:24
j Hes 32:5
k Hes 32:25

Safu ya 2
a Yos 4:13
b Yos 1:15
2Fa 10:33
c Kum 3:12
d Yos 13:8
e Kum 29:8
Yos 12:6
Yos 22:7
1Nya 5:18
f Hes 21:23
Hes 21:24
Kum 2:31
Zb 136:19
g Kum 3:4
Zb 135:11
h Hes 21:30
Hes 33:45
Yos 13:17
i Hes 32:3
j Kum 2:36
Yos 12:2
Amu 11:26
k Hes 21:32
Yos 13:25
l Amu 8:11
m Hes 32:3
n Yos 13:27
o Hes 32:17
p Hes 32:24
q Hes 21:26
Yos 13:17
r Hes 32:3
Yer 48:34
s Yos 13:19
t Hes 32:3
u Yos 13:17
Eze 25:9
v Hes 26:29
w Kum 3:13
Yos 13:31
Yos 17:1
x Kum 3:14
Yos 13:30
y 1Nya 2:23

SURA 33
z Kut 12:51
a Kut 13:18
b Yos 24:5
1Sa 12:8
Zb 77:20
Mik 6:4

Musa akaendelea kuandika ma-
hali walipoondoka, kulingana
na vituo vyao kwa agizo la Ye-
hova; navyo hivi ndivyo vilivyo-
kuwa vituo vyao kutoka maha-
li pamoja walipoondoka mpaka
pengine:[a] **3** Nao wakaondo-
ka Ramesesi[b] katika mwezi wa
kwanza, katika siku ya kumi
na tano ya mwezi wa kwa-
nza.[c] Siku ileile iliyofuata pa-
saka[d] wana wa Israeli wakato-
ka kwa mkono ulioinuliwa mbe-
le ya macho ya Wamisri wote.[e]
4 Wakati wote huo, Wamisri
walikuwa wakiwazika wale
ambao Yehova alikuwa amewa-
piga katikati yao, yaani, wazali-
wa wote wa kwanza;[f] na juu
ya miungu yao Yehova alikuwa
amefanya hukumu.[g]

5 Kwa hiyo wana wa Israe-
li wakaondoka Ramesesi,[h] wa-
kapiga kambi Sukothi.[i] **6** Ki-
sha wakaondoka Sukothi, wa-
kapiga kambi Ethamu,[j] amba-
po pako ukingoni mwa nyika.
7 Halafu wakaondoka Etha-
mu, wakageuka na kurudi nyu-
ma kuelekea Pihahirothi,[k]
ambapo panaelekeana na Baal-
sefoni;[l] nao wakapiga kambi
mbele ya Migdoli.[m] **8** Halafu
wakaondoka Pihahirothi, wa-
kapita katikati ya bahari[n] mpa-
ka nyikani,[o] wakaendelea kupi-
ga mwendo safari ya siku tatu
katika nyika ya Ethamu,[p] wa-
kapiga kambi Mara.[q]

9 Kisha wakaondoka Mara
wakaja Elimu.[r] Sasa katika Eli-
mu kulikuwa na mabubujiko 12
ya maji na mitende 70. Kwa
hiyo wakapiga kambi huko.
10 Kisha wakaondoka Elimu,
wakapiga kambi kando ya Ba-
hari Nyekundu. **11** Baada ya
hapo wakaondoka katika Baha-
ri Nyekundu, wakapiga kambi
katika nyika ya Sini.[s] **12** Ha-

SURA 33

a Hes 9:17
b Mwa 47:11
Kut 12:37
c Kut 12:2
Kut 13:4
d Kut 12:6
Hes 9:3
Kum 16:1
e Kut 14:8
f Kut 12:29
Zb 78:51
g Kut 12:12
Kut 18:11
h Mwa 47:11
i Kut 12:37
j Kut 13:20
k Kut 14:2
l Kut 14:9
m Kut 14:2
n Kut 14:22
Zb 106:9
Ebr 11:29
o Kut 15:22
p Kut 13:20
q Kut 15:23
r Kut 15:27
s Kut 16:1

Safu ya 2

a Kut 17:1
Kut 17:8
b Kut 18:5
Kut 19:1
Kut 19:2
Hes 1:1
Hes 3:4
Hes 9:1
c Hes 11:34
Kum 9:22
d Hes 11:35
Hes 12:16
Kum 1:1
e Hes 2:3
Hes 2:10
Hes 2:18
Hes 2:25
Hes 2:34
f Hes 9:17
g Kum 10:6

lafu wakaondoka katika nyika
ya Sini, wakapiga kambi Dof-
ka. **13** Baadaye wakaondoka
Dofka, wakapiga kambi Alushi.
14 Kisha wakaondoka Alushi,
wakapiga kambi Refidimu.[a] Na
huko kukawa hakuna maji ya
kunywa kwa ajili ya watu.
15 Baada ya hapo wakaondoka
Refidimu, wakapiga kambi ka-
tika nyika ya Sinai.[b]

16 Halafu wakaondoka kati-
ka nyika ya Sinai, wakapiga ka-
mbi Kibroth-hataava.[c] **17** Ki-
sha wakaondoka Kibroth-
hataava, wakapiga kambi Ha-
serothi.[d] **18** Baada ya hapo
wakaondoka Haserothi, wa-
kapiga kambi Rithma. **19** Ki-
sha wakaondoka Rithma, wa-
kapiga kambi Rimon-peresi.
20 Halafu wakaondoka Rimon-
peresi, wakapiga kambi Libna.
21 Baadaye wakaondoka Li-
bna, wakapiga kambi Risa.
22 Kisha wakaondoka Risa,
wakapiga kambi Kehelatha.
23 Halafu wakaondoka Kehe-
latha, wakapiga kambi katika
Mlima Sheferi.

24 Baada ya hapo waka-
ondoka Mlima Sheferi, wakapi-
ga kambi[e] Harada. **25** Halafu
wakaondoka Harada, wakapi-
ga kambi Makelothi. **26** Kisha
wakaondoka[f] Makelothi, waka-
piga kambi Tahathi. **27** Baada
ya hapo wakaondoka Tahathi,
wakapiga kambi Tera. **28** Ha-
lafu wakaondoka Tera, waka-
piga kambi Mithka. **29** Baada-
ye wakaondoka Mithka, wakapi-
ga kambi Hashmona. **30** Ki-
sha wakaondoka Hashmona,
wakapiga kambi Moserothi.
31 Halafu wakaondoka Mosero-
thi, wakapiga kambi Bene-yaa-
kani.[g] **32** Baada ya hapo waka-
ondoka Bene-yaakani, wakapiga

kambi Hor-hagidgadi. **33** Kisha wakaondoka Hor-hagidgadi, wakapiga kambi Yotbata.[a] **34** Baadaye wakaondoka Yotbata, wakapiga kambi Abrona. **35** Halafu wakaondoka Abrona, wakapiga kambi Esion-geberi.[b] **36** Baada ya hapo wakaondoka Esion-geberi, wakapiga kambi katika nyika ya Zini,[c] yaani, Kadeshi.

37 Baadaye wakaondoka Kadeshi, wakapiga kambi katika Mlima Hori,[d] kwenye mpaka wa nchi ya Edomu. **38** Naye Haruni kuhani akapanda katika Mlima Hori kwa agizo la Yehova, akafa huko katika mwaka wa 40 tangu wana wa Israeli walipotoka katika nchi ya Misri, katika mwezi wa 5, siku ya kwanza ya mwezi huo.[e] **39** Naye Haruni alikuwa na umri wa miaka 123 alipokufa kwenye Mlima Hori.

40 Sasa yule Mkanaani, mfalme wa Aradi,[f] alipokuwa akikaa katika Negebu,[g] katika nchi ya Kanaani, akapata kusikia juu ya kuja kwa wana wa Israeli.

41 Baada ya muda wakaondoka katika Mlima Hori,[h] wakapiga kambi Salmona. **42** Baada ya hapo wakaondoka Salmona, wakapiga kambi Punoni. **43** Kisha wakaondoka Punoni, wakapiga kambi Obothi.[i] **44** Halafu wakaondoka Obothi, wakapiga kambi Iye-abarimu kwenye mpaka wa Moabu.[j] **45** Baadaye wakaondoka Iyimu, wakapiga kambi Dibon-gadi.[k] **46** Baada ya hapo wakaondoka Dibon-gadi, wakapiga kambi Almon-diblathaimu. **47** Halafu wakaondoka Almon-diblathaimu,[l] wakapiga kambi katika milima ya Abarimu[a] mbele ya Nebo.[b] **48** Mwishowe wakaondoka katika milima ya Abarimu, wakapiga kambi katika nchi tambarare za jangwa la Moabu[c] kando ya Yordani, kule Yeriko. **49** Nao wakaendelea kukaa katika kambi kando ya Yordani kutoka Beth-yeshimothi[d] mpaka Abel-shitimu[e] katika nchi tambarare za jangwa la Moabu.

50 Na Yehova akasema na Musa katika nchi tambarare za jangwa la Moabu kando ya Yordani, kule Yeriko,[f] na kumwambia: **51** "Sema na wana wa Israeli, nawe utawaambia, 'Mtavuka Yordani kuingia katika nchi ya Kanaani.[g] **52** Nanyi mnapaswa kuwafukuzia mbali wakaaji wote wa nchi hiyo kutoka mbele yenu na kuharibu maumbo yao yote ya mawe,[h] nanyi mnapaswa kuziharibu sanamu zao zote za madini ya kuyeyusha,[i] na mnapaswa kupaharibu mahali pao pote patakatifu.[j] **53** Nanyi mtaimiliki nchi na kukaa humo, kwa sababu hakika nitawapa ninyi nchi hiyo mpate kuimiliki.[k] **54** Nanyi mtaigawa nchi hiyo kwa ajili yenu iwe miliki kwa kura[l] kulingana na familia zenu.[m] Kwake aliye na hesabu kubwa mtaongeza urithi wake, na kwake aliye mchache mtaupunguza urithi wake.[n] Mahali ambapo kura itamtokea, hapo patakuwa pake.[o] Kulingana na makabila ya baba zenu mnapaswa kumiliki nchi.[p]

55 "'Hata hivyo, ikiwa hamtawafukuzia mbali wakaaji wa nchi hiyo kutoka mbele yenu,[q] basi wale mtakaoacha watakuwa kama michomo katika macho yenu na kama miiba ubavuni mwenu, nao watawasumbua katika nchi amba-

SURA 33

a Kum 10:7
b Kum 2:8
1Fa 9:26
2Nya 8:17
c Hes 13:21
Hes 14:25
Hes 20:1
Hes 27:14
Kum 32:51
Yos 15:1
d Hes 20:22
Hes 20:23
Kum 32:50
e Kum 10:6
f Hes 21:1
Amu 1:16
g Hes 13:17
Yos 10:40
h Hes 21:4
i Hes 21:10
j Mwa 19:37
Hes 21:11
Hes 21:13
k Hes 21:30
Hes 32:34
l Yer 48:22

Safu ya 2

a Hes 27:12
Kum 32:49
b Kum 34:1
c Hes 22:1
d Yos 12:3
Yos 13:20
e Hes 25:1
Yos 2:1
Mik 6:5
f Hes 22:1
Yos 2:2
Ebr 11:30
g Kum 7:1
Kum 9:1
Yos 3:17
h Law 26:1
i Kut 34:17
Law 19:4
Kum 27:15
j Kut 23:24
Kut 34:13
Kum 7:5
Kum 12:3
k Kum 32:8
Yer 27:5
Da 4:35
l Met 16:33
m Hes 26:53
n Hes 26:54
o Yos 15:1
p Yos 16:1
Yos 18:11
q Amu 1:21
Zb 106:34

mo mtakuwa mkikaa.[a] **56** Na itatukia kwamba kama vile nilivyokusudia kuwatendea hao, ndivyo nitakavyowatendea ninyi.'"[b]

34 Na Yehova akazidi kusema na Musa, na kumwambia: **2** "Waamuru wana wa Israeli, nawe utawaambia, 'Mnaingia katika nchi ya Kanaani.[c] Hiyo ndiyo nchi itakayowaangukia kwa urithi,[d] nchi ya Kanaani kulingana na mipaka yake.[e]

3 "'Na upande wenu wa kusini utakuwa kutoka nyika ya Zini kando ya Edomu,[f] nao mpaka wenu wa kusini utakuwa kutoka mwisho wa Bahari ya Chumvi[g] upande wa mashariki. **4** Nao mpaka wenu utabadilika kutoka kusini mwa mpando wa Akrabimu[h] na kuvuka hadi Zini, nao mwisho wake utakuwa kusini mwa Kadesh-barnea;[i] nao utatoka Hasar-adari[j] na kuvuka hadi Asimoni. **5** Nao mpaka utabadilika hapo Asimoni hadi kwenye bonde la mto la Misri,[k] na mwisho wake utakuwa katika ile Bahari.[l]

6 "'Nao mpaka wenu wa magharibi,[m] utakuwa Bahari Kuu na nchi ya pwani. Huo utakuwa mpaka wenu wa magharibi.

7 "'Sasa huu ndio utakuwa mpaka wenu wa kaskazini: Kutoka Bahari Kuu mtatia alama kufika Mlima Hori[n] uwe mpaka wenu. **8** Kutoka Mlima Hori mtatia mpaka alama hadi mahali pa kuingilia pa Hamathi,[o] na mwisho wa mpaka utakuwa Sedadi.[p] **9** Nao mpaka utaenda hadi Zifroni, nao mwisho wake utakuwa Hasar-enani.[q] Huo utakuwa mpaka wenu wa kaskazini.

SURA 33
a Kut 23:33; Kum 7:4; Yos 23:13; Amu 2:3; Zb 106:36
b Law 18:28; Yos 23:15

SURA 34
c Mwa 15:18; Mwa 17:8; Zb 105:11
d Kum 4:38; Yos 1:4; Yos 14:1; Yer 3:19
e Mwa 10:19; Mdo 17:26
f Yos 15:1
g Mwa 14:3; Yos 15:2
h Amu 1:36
i Hes 13:26; Hes 32:8
j Yos 15:3
k Yos 15:4; Yos 15:47
l Kut 23:31
m Yos 1:4; Yos 15:12
n Hes 33:37; Kum 32:50
o Hes 13:21; 2Fa 14:25
p Eze 47:15
q Eze 47:17

Safu ya 2
a Kum 3:17; Yos 11:2; Lu 5:1; Yoh 6:1
b Yos 15:2
c Kum 8:7
d Hes 26:55; Hes 33:54; Yos 14:2; Yos 18:6; Met 16:33
e Yos 14:2
f Hes 32:33; Kum 3:12; Kum 3:13; Yos 13:8
g Hes 32:5; Hes 32:32
h Hes 3:32; Hes 20:26; Yos 14:1; Yos 19:51
i Hes 14:38; Hes 27:18
j Hes 1:4; Hes 1:16
k Yos 15:1
l Hes 14:30; Hes 26:65
m Yos 19:1

10 "'Halafu mtatia alama mpaka wenu wa mashariki kutoka Hasar-enani hadi Shefamu. **11** Na mpaka huo utashuka kutoka Shefamu hadi Ribla upande wa mashariki wa Aini, nao mpaka utashuka hadi mteremko wa mashariki wa bahari ya Kinerethi.[a] **12** Nao mpaka utashuka hadi Yordani, na mwisho wake utakuwa katika Bahari ya Chumvi.[b] Hiyo itakuwa nchi[c] yenu kulingana na mipaka yake kuizunguka pande zote.'"

13 Kwa hiyo Musa akawaamuru wana wa Israeli, na kusema: "Hii ndiyo nchi mtakayojigawia kwa kura[d] iwe miliki, kama vile ambavyo Yehova ameamuru ili kuyapa yale makabila tisa na nusu.[e] **14** Kwa maana kabila la wana wa Warubeni kulingana na nyumba za baba zao na kabila la wana wa Wagadi kulingana na nyumba za baba zao tayari wamechukua, na nusu ya kabila la Manase tayari wamechukua urithi wao.[f] **15** Yale makabila mawili na nusu tayari yamechukua urithi wao kutoka katika eneo la Yordani kando ya Yeriko upande wa mashariki kuelekea mashariki."[g]

16 Na Yehova akazidi kusema na Musa, na kumwambia: **17** "Haya ndiyo majina ya wanaume watakaowagawia ninyi nchi iwe miliki, Eleazari[h] kuhani na Yoshua mwana wa Nuni.[i] **18** Nanyi mtachukua mkuu mmoja kutoka katika kila kabila ili kuigawa nchi iwe miliki.[j] **19** Nayo haya ndiyo majina ya wanaume hao: Wa kabila la Yuda,[k] Kalebu mwana wa Yefune;[l] **20** na wa kabila la wana wa Simeoni,[m] Shemueli mwana wa Amihudi; **21** wa

kabila la Benyamini,[a] Elidadi
mwana wa Kisloni; **22** na wa
kabila la wana wa Dani,[b] mkuu
mmoja, Buki mwana wa Yogli;
23 wa wana wa Yosefu,[c] wa ka-
bila la wana wa Manase,[d] mkuu
mmoja, Hanieli mwana wa Efo-
di; **24** na wa kabila la wana
wa Efraimu,[e] mkuu mmoja,
Kemueli mwana wa Shiftani;
25 na wa kabila la wana wa Za-
buloni,[f] mkuu mmoja, Elisafa-
ni mwana wa Parnaki; **26** na
wa kabila la wana wa Isakari,[g]
mkuu mmoja, Paltieli mwana
wa Azani; **27** na wa kabila la
wana wa Asheri,[h] mkuu mmo-
ja, Ahihudi mwana wa Shelo-
mi; **28** na wa kabila la wana
wa Naftali,[i] mkuu mmoja, Pe-
daheli mwana wa Amihudi."
29 Hao ndio watu ambao Ye-
hova aliwaamuru wawafanye
wana wa Israeli waimiliki nchi
katika nchi ya Kanaani.[j]

35 Na Yehova akaendelea
kusema na Musa kwe-
nye nchi tambarare za jangwa
la Moabu kando ya Yordani,[k]
huko Yeriko, na kumwambia:
2 "Wape wana wa Israeli amri
ya kwamba lazima wawape Wa-
lawi majiji[l] wakae humo kutoka
katika urithi wa miliki yao, nao
watawapa Walawi kiwanja cha
malisho cha majiji kuzunguka
pande zote.[m] **3** Na majiji hayo
yatatumika kwao kuwa ma-
kao yao, navyo viwanja vyao
vya malisho vitakuwa kwa aji-
li ya wanyama wao wa kufu-
gwa na mali zao na kwa aji-
li ya wanyama-mwitu wao wote.
4 Na viwanja vya malisho vya
majiji hayo, ambayo mtawapa
Walawi, vitakuwa kutoka kati-
ka ukuta wa jiji kuelekea nje ki-
pimo cha mikono elfu moja ku-
zunguka pande zote. **5** Nanyi

SURA 34

a Yos 18:11
b Yos 19:40
c Mwa 46:20
Mwa 48:5
Yos 16:1
d Yos 17:1
e Yos 16:5
f Yos 19:10
g Yos 19:17
h Yos 19:24
i Yos 19:32
j Hes 34:18
Kum 32:8
Yos 19:51
Mdo 17:26

SURA 35

k Hes 22:1
Hes 31:12
Hes 36:13
l Mwa 49:7
Law 25:32
Kum 18:1
Yos 14:4
Yos 21:2
m Law 25:34
Yos 21:3
Yos 21:11
1Nya 6:64
2Nya 11:14

Safu ya 2

a Hes 35:13
Yos 20:2
Yos 20:7
Yos 20:8
Yos 21:13
Yos 21:21
Yos 21:27
Yos 21:32
Yos 21:36
Yos 21:38
b Kum 4:41
Kum 4:42
Yos 20:3
c Yos 21:3
d Mwa 49:7
e Hes 26:54
Hes 33:54
f Kut 3:8
Kut 23:23
Hes 34:2
g Kut 21:13
Kum 4:42
Kum 19:4
h Hes 35:19
Kum 19:6
Yos 20:9
i Kum 19:11
Kum 19:12
Yos 20:5
j Kum 4:41
Kum 19:9

mtapima nje ya jiji upande wa
mashariki mikono elfu mbili na
upande wa kusini mikono elfu
mbili na upande wa magharibi
mikono elfu mbili na upande
wa kaskazini mikono elfu mbi-
li, jiji likiwa katikati. Hicho ki-
tatumika kwao kama kiwanja
cha malisho cha majiji hayo.

6 "Haya ndiyo majiji mtaka-
yowapa Walawi: majiji 6 ya ma-
kimbilio,[a] ambayo mtatoa ili
muuaji akimbilie humo,[b] na
mbali na hayo mtatoa maji-
ji mengine 42. **7** Majiji yote
mtakayowapa Walawi yataku-
wa majiji 48, hayo pamoja na
viwanja vyake vyote vya mali-
sho.[c] **8** Majiji mtakayotoa ya-
tatoka katika miliki ya wana
wa Israeli.[d] Kutoka kwa wengi
mtachukua mengi, na kutoka
kwa wachache mtachukua ma-
chache.[e] Kila mmoja kulinga-
na na urithi wake atakaochu-
kua uwe miliki, atawapa Wala-
wi sehemu ya majiji yake."

9 Naye Yehova akaendelea
kusema na Musa, na ku-
mwambia: **10** "Sema na wana
wa Israeli, nawe utawaam-
bia, 'Mtavuka Yordani na ku-
ingia katika nchi ya Kanaa-
ni.[f] **11** Nanyi mtachagua ma-
jiji yatakayowafaa ninyi. Yata-
tumika kwenu yakiwa majiji
ya makimbilio, naye muuaji
atakayeipiga nafsi na kuiua
bila kukusudia lazima akimbi-
lie humo.[g] **12** Na majiji hayo
yatatumika kwenu yakiwa ma-
kimbilio ili kumkimbia mlipiza-
kisasi cha damu,[h] kusudi muu-
aji asife mpaka asimame mbele
ya kusanyiko kwa ajili ya huku-
mu.[i] **13** Nayo majiji mtakayo-
toa, yale majiji sita ya makimbi-
lio, yatakuwa kwa ajili yenu.
14 Mtatoa majiji matatu upa-
nde huu wa Yordani,[j] na maji-

ji matatu mtatoa katika nchi ya Kanaani.[a] Yatatumika yakiwa majiji ya makimbilio. **15** Majiji hayo sita yatatumika yakiwa kimbilio kwa wana wa Israeli na kwa mkaaji mgeni[b] na kwa mhamiaji aliye kati yao, ili mtu yeyote ambaye ataipiga nafsi na kuiua bila kukusudia akimbilie humo.[c]

16 "'Sasa ikiwa amempiga kwa chombo cha chuma akafa, yeye ni muuaji wa kukusudia.[d] Lazima muuaji huyo wa kukusudia auawe.[e] **17** Na ikiwa alimpiga kwa jiwe dogo ambalo lingeweza kumuua naye afe, yeye ni muuaji wa kukusudia. Lazima muuaji huyo wa kukusudia auawe. **18** Na ikiwa alimpiga kwa chombo kidogo cha mbao ambacho kingeweza kumuua naye afe, yeye ni muuaji wa kukusudia. Lazima muuaji huyo wa kukusudia auawe.

19 "'Mlipiza-kisasi[f] cha damu ndiye atakayemuua huyo muuaji wa kukusudia. Hapo atakapokutana naye atamuua. **20** Na ikiwa alikuwa akimsukuma[g] kwa sababu ya chuki au ikiwa amemvizia[h] na kumtupia kitu ili afe, **21** au ikiwa kwa uadui amempiga kwa mkono wake ili afe, lazima mpigaji huyo atauawa. Yeye ni muuaji wa kukusudia. Mlipiza-kisasi cha damu atamuua yule muuaji wa kukusudia akimkuta.[i]

22 "'Lakini ikiwa alimsukuma bila uadui wowote au kumtupia chombo chochote pasipo kumvizia,[j] **23** au jiwe lolote ambalo lingeweza kumuua pasipo yeye kumwona, au kumwangushia, naye afe, naye hakuwa adui yake wala hakuwa akitafuta kumdhuru, **24** ndipo kusanyiko litahukumu kati ya yule mpigaji na yule mlipiza-kisasi cha damu kulingana na hukumu hizi.[a] **25** Nalo kusanyiko[b] lazima limkomboe muuaji asiyekusudia kutoka mkononi mwa mlipiza-kisasi cha damu, nalo kusanyiko litamrudisha katika jiji lake la makimbilio alilokuwa amekimbilia, naye atakaa humo mpaka kifo cha kuhani mkuu aliyetiwa mafuta kwa kutumia mafuta matakatifu.[c]

26 "'Lakini ikiwa muuaji asiyekusudia atatoka nje ya mipaka ya jiji la makimbilio ambalo amekimbilia, **27** naye mlipiza-kisasi[d] cha damu amkute nje ya mpaka wa lile jiji la makimbilio, na yule mlipiza-kisasi cha damu amuue yule muuaji asiyekusudia, yeye hana hatia ya damu. **28** Kwa maana alipaswa kukaa katika jiji la makimbilio mpaka kifo cha kuhani mkuu,[e] na baada ya kifo cha kuhani mkuu yule muuaji asiyekusudia anaweza kurudi katika nchi iliyo miliki yake. **29** Nazo hizo zitatumika kuwa sheria za hukumu kwa ajili yenu katika vizazi vyenu vyote katika makao yenu yote.

30 "'Kila mwenye kupiga nafsi na kuiua anapaswa kuuawa akiwa muuaji wa kukusudia[f] kwa kinywa cha mashahidi,[g] na shahidi mmoja hawezi kutoa ushuhuda juu ya nafsi ili afe. **31** Nanyi hampaswi kuchukua fidia kwa ajili ya nafsi ya muuaji wa kukusudia anayestahili kufa,[h] kwa maana lazima auawe.[i] **32** Nanyi hampaswi kuchukua fidia kwa ajili ya mtu ambaye amekimbia kwenda katika jiji lake la makimbilio, ili arudi kukaa katika nchi kabla ya kifo cha kuhani mkuu.

SURA 35

a Yos 20:7
b Kut 12:49
Law 19:34
Law 24:22
Hes 15:16
c Yos 20:3
d Kum 19:11
e Mwa 9:5
Kut 21:12
Law 24:17
Kum 19:12
f Hes 35:12
Kum 19:6
g Mwa 4:8
2Sa 20:10
h Kut 21:14
Kum 19:11
Zb 10:8
Met 1:18
Mk 6:19
Mdo 23:21
i Hes 35:19
j Kut 21:13
Kum 19:5
Yos 20:3
Yos 20:5

Safu ya 2

a Hes 35:12
Yos 20:4
b Amu 20:13
c Kut 29:7
Law 21:10
Ebr 3:1
d Hes 35:12
Hes 35:19
e Yos 20:6
f Mwa 9:6
Kut 20:13
Kum 5:17
g Kum 17:6
Kum 19:15
Mt 18:16
Yoh 8:17
2Ko 13:1
1Ti 5:19
Ebr 10:28
h 1Yo 3:15
i Mwa 9:5
Kut 21:14
Kum 19:13

33 "'Nanyi msiichafue nchi mliyo ndani yake; kwa sababu damu ndiyo inayoichafua nchi,[a] na kwa ajili ya nchi hakuwezi kuwa na upatanisho kuhusu damu ambayo imemwagwa juu yake isipokuwa kwa damu ya yule anayeimwaga.[b] **34** Wala msiitie unajisi nchi ambayo mnakaa ndani yake, ambayo mimi ninakaa katikati yake; kwa maana mimi Yehova ninakaa katikati ya wana wa Israeli.'"[c]

36 Nao vichwa vya upande wa baba vya familia ya wana wa Gileadi mwana wa Makiri[d] mwana wa Manase wa familia za wana wa Yosefu wakakaribia na kusema mbele ya Musa na wakuu, vichwa vya upande wa baba vya wana wa Israeli, **2** na kusema: "Yehova alimwamuru bwana wangu awape wana wa Israeli nchi iwe urithi kwa kura;[e] naye bwana wangu aliamriwa na Yehova kwamba urithi wa Selofehadi ndugu yetu awape binti zake.[f] **3** Ikiwa yeyote wa wana wa yale makabila mengine ya wana wa Israeli atawachukua wawe wake zao, urithi wa wanawake hao utaondolewa pia kutoka katika urithi wa baba zetu na kuongezwa katika urithi wa kabila watakaloingia, hivi kwamba utaondolewa katika kura ya urithi wetu.[g] **4** Sasa Yubile[h] ikitukia kwa ajili ya wana wa Israeli, urithi wa wanawake hao utaongezwa kwenye urithi wa kabila watakaloingia; hivi kwamba urithi wao utaondolewa katika urithi wa kabila la baba zetu."

5 Ndipo Musa akawaamuru wana wa Israeli kwa agizo la Yehova, na kusema: "Kabila la wana wa Yosefu linasema jambo lililo sawa. **6** Hili ndilo neno ambalo Yehova ameamuru kwa ajili ya binti za Selofehadi,[a] na kusema, 'Kwa yeyote atakayekuwa mwema machoni pao wanaweza kuwa wake zake. Ila tu wanapaswa kuwa wake katika familia ya kabila la baba zao.[b] **7** Na hakuna urithi wowote wa wana wa Israeli unaopaswa kuzunguka kutoka kabila moja mpaka kabila lingine, kwa sababu wana wa Israeli wanapaswa kushikamana kila mmoja wao na urithi wa kabila la mababu zake. **8** Na kila binti atakayepata miliki ya urithi kutoka katika makabila ya wana wa Israeli, anapaswa kuwa mke katika mojawapo ya familia za kabila la baba yake,[c] ili wana wa Israeli wapate miliki kila mmoja katika urithi wa mababu zake. **9** Wala hakuna urithi unaopaswa kuzunguka kutoka katika kabila moja mpaka lingine, kwa sababu makabila ya wana wa Israeli yanapaswa kushikamana kila mmoja na urithi wake mwenyewe.'"

10 Kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa, hivyo ndivyo binti za Selofehadi walivyofanya.[d] **11** Basi Mala, Tirsa na Hogla na Milka na Noa, binti za Selofehadi,[e] wakawa wake za wana wa ndugu za baba yao. **12** Wakawa wake za baadhi ya familia za wana wa Manase mwana wa Yosefu, ili urithi wao uendelee kuwa pamoja na kabila la familia ya baba yao.

13 Hizi ndizo amri[f] na maamuzi ya hukumu ambayo Yehova aliwaamuru wana wa Israeli kupitia Musa, katika nchi tambarare za jangwa la Moabu kando ya Yordani, huko Yeriko.[g]

SURA 35
a Mwa 4:10; Zb 106:38; Lu 11:50
b Mwa 9:6
c Kut 25:8; Kut 29:46; Law 26:12; 1Fa 6:13

SURA 36
d Hes 26:29; Yos 17:1
e Hes 26:55; Hes 33:54
f Hes 27:1; Hes 27:7
g Hes 27:4
h Law 25:10

Safu ya 2
a Hes 36:2
b Hes 36:12
c 1Nya 23:22
d Hes 36:6
e Hes 27:1
f Kum 30:8; Yos 22:5; Mhu 12:13
g Hes 26:3; Hes 33:50; Hes 35:1

KUMBUKUMBU LA TORATI

1 Haya ndiyo maneno ambayo Musa aliwaambia Israeli wote katika eneo la Yordani[a] nyikani, katika nchi tambarare za jangwa mbele ya Sufi, katikati ya Parani[b] na Tofeli na Labani na Haserothi[c] na Dizahabu, **2** mwendo wa siku kumi na moja kutoka Horebu kupitia njia ya Mlima Seiri mpaka Kadesh-barnea.[d] **3** Na ikawa kwamba katika mwaka wa 40,[e] katika mwezi wa kumi na moja, siku ya kwanza ya mwezi huo, Musa akasema na wana wa Israeli kulingana na yote ambayo Yehova alikuwa amemwamuru kwa ajili yao, **4** baada ya kumshinda Sihoni[f] mfalme wa Waamori, aliyekuwa akikaa kule Heshboni, na Ogu[g] mfalme wa Bashani, aliyekuwa akikaa kule Ashtarothi,[h] katika Edrei.[i] **5** Katika eneo la Yordani nchini Moabu, Musa akaanza kuifafanua sheria hii,[j] na kusema:

6 "Yehova Mungu wetu alisema nasi katika Horebu,[k] na kutuambia hivi, 'Mmekaa muda mrefu vya kutosha katika eneo hili lenye milima.[l] **7** Geukeni mfunge safari, mwende kwenye eneo lenye milima la Waamori[m] na kwa jirani zao wote katika Araba,[n] lile eneo lenye milima[o] na Shefela na Negebu[p] na pwani ya bahari,[q] nchi ya Wakanaani,[r] na Lebanoni,[s] mpaka ule mto mkubwa, mto Efrati.[t] **8** Tazama, naiweka nchi hiyo mbele yenu. Ingieni mwimiliki nchi ambayo Yehova aliwaapia baba zenu, Abrahamu, Isaka[u] na Yakobo,[v] kwamba atawapa wao na uzao wao baada yao.'[w]

SURA 1

a Yos 22:4
b Hes 10:12
c Hes 33:18
d Hes 13:26
Kum 9:23
Yos 14:7
e Hes 32:13
Hes 33:38
f Hes 21:23
Yos 12:2
g Hes 21:33
Ne 9:22
Zb 135:11
h Yos 9:10
i Yos 13:12
j Kum 4:8
Kum 17:18
Ne 8:7
k Kum 4:15
1Fa 8:9
l Kut 19:1
Hes 10:11
Hes 10:12
m Mwa 15:16
Yos 10:6
n Kum 3:17
Kum 4:49
Yos 12:3
o Hes 13:17
p Mwa 12:9
Hes 21:1
q Yos 9:1
r Hes 34:2
s Yos 13:1
Yos 13:5
1Fa 9:19
t Mwa 15:18
u Mwa 26:3
v Mwa 28:13
w Mwa 12:7
Mwa 13:15
Mwa 17:7

Safu ya 2

a Kut 18:18
b Mwa 15:5
Kut 32:13
Hes 26:51
Kum 10:22
c 1Fa 3:8
1Nya 27:23
Zb 115:14
d Mwa 26:4
Kut 23:25
Met 10:22
e Mwa 12:2
Mwa 22:17
f Kut 18:18
Hes 11:11
Hes 20:3
Hes 27:14
g 1Ti 3:2
h 1Ti 3:4
1Ti 3:6
i Kut 18:21
j Kut 18:25
k Kut 23:8
Kum 16:18
Yoh 7:24
l Kut 22:21
Law 19:34
Law 24:22

9 "Nami nikawaambia hivi wakati huo, 'Mimi peke yangu siwezi kuwabeba ninyi.[a] **10** Yehova Mungu wenu amewazidisha ninyi, na tazama, ninyi leo ni kama nyota za mbinguni kwa wingi.[b] **11** Yehova Mungu wa mababu zenu na awaongeze[c] mara elfu moja zaidi ya jinsi mlivyo, naye na awabariki[d] ninyi kama vile alivyowaahidi ninyi.[e] **12** Mimi peke yangu ninawezaje kuubeba uzito wenu na mzigo wenu na ugomvi wenu?[f] **13** Tafuteni watu wenye hekima na busara[g] na uzoefu[h] wa makabila yenu, ili niwaweke wawe vichwa juu yenu.'[i] **14** Ndipo mkanijibu na kusema, 'Jambo ambalo umesema tufanye ni jema.' **15** Basi nikawachukua vichwa vya makabila yenu, wanaume wenye hekima na uzoefu, na kuwaweka kuwa vichwa juu yenu, wakuu wa maelfu na wakuu wa mamia na wakuu wa 50 na wakuu wa makumi na maofisa wa makabila yenu.[j]

16 "Nami nikawaamuru waamuzi wenu wakati huo, na kusema, 'Mnaposikiliza kesi kati ya ndugu zenu, hukumuni kwa uadilifu[k] kati ya mtu na ndugu yake au mkaaji mgeni wake.[l] **17** Msipendelee katika hukumu.[m] Msikilizeni mdogo sawa na mkubwa.[n] Msiogope kwa sababu ya mwanadamu,[o] kwa maana hukumu ni ya Mungu;[p] na kesi ambayo ni ngumu mno kwenu, nileteeni, nami nitaisikiliza.'[q] **18** Nami

m Law 19:15; 1Sa 16:7; Met 24:23; Lu 20:21; Ro 2:11; n Kut 23:3; Yak 2:4; o Met 29:25; p 2Nya 19:6; q Kut 18:26.

nikawaamuru ninyi wakati huo
mambo yote mnayopaswa kufa-
nya.
19 "Halafu tukaondoka Ho-
rebu na kupiga mwendo kupitia
nyika yote hiyo iliyo kuu na ye-
nye kutia woga,[a] ambayo mmei-
ona, kupitia eneo lenye milima
la Waamori,[b] kama vile Yehova
Mungu wetu alivyokuwa ame-
tuamuru; na mwishowe tukafi-
ka Kadesh-barnea.[c] **20** Sasa
nikawaambia ninyi, 'Mmefika
kwenye eneo lenye milima la
Waamori, ambalo Yehova Mu-
ngu wetu anatupa sisi.[d] **21** Ta-
zama, Yehova Mungu wako ame-
itia nchi hiyo mikononi mwako.[e]
Panda, ukaimiliki, kama vile Ye-
hova Mungu wa mababu zako
alivyokuambia.[f] Usiogope, wala
usiingiwe na hofu.'[g]
22 "Hata hivyo, ninyi nyo-
te mkanikaribia na kusema,
'Acha tutume watu mbele yetu,
wakaipeleleze nchi kwa aji-
li yetu, watuletee neno kuhu-
su njia ambayo tutaipitia kwe-
nda katika majiji tutakayo-
yafikia.'[h] **23** Basi, jambo hilo
likawa jema machoni pangu,
hivi kwamba nikachukua wa-
naume kumi na wawili kati
yenu, mmoja kwa ajili ya kila
kabila.[i] **24** Kisha wakageu-
ka na kupanda eneo lenye mi-
lima,[j] wakafika kwenye bonde
la mto la Eshkoli,[k] wakape-
leleza. **25** Nao wakachukua
sehemu ya matunda ya nchi[l]
hiyo mkononi mwao na kutu-
letea, nao wakaja na kutuletea
neno na kusema, 'Nchi amba-
yo Yehova Mungu wetu ana-
tupa sisi ni nzuri.'[m] **26** Laki-
ni hamkutaka kwenda,[n] na-
nyi mkaanza kujiendesha kwa
kuliasi agizo la Yehova Mu-
ngu wenu.[a] **27** Nanyi mkanu-
ng'unika katika mahema yenu
na kusema, 'Kwa sababu Yeho-
va alituchukia,[b] ndiyo maana
alitutoa katika nchi ya Misri[c]
atutie mkononi mwa Waamo-
ri, ili kutuangamiza.[d] **28** Tu-
napanda kwenda wapi? Ndugu
zetu wameufanya moyo wetu
uyeyuke,[e] kwa kusema: "Tuli-
ona huko watu wakubwa zai-
di na warefu zaidi kuliko sisi,[f]
majiji makubwa na yaliyotiwa
ngome mpaka mbinguni[g] na pia
wale wana wa Waanaki."'[h]
29 "Kwa hiyo nikawaambia
ninyi, 'Msishtuke wala kuogo-
pa kwa sababu yao.[i] **30** Yeho-
va Mungu wenu ndiye anayee-
nda mbele yenu. Atawapigania
ninyi[j] kulingana na yote amba-
yo aliwafanyia ninyi katika Mi-
sri chini ya macho yenu wenye-
we,[k] **31** na katika nyika,[l] ma-
hali ambapo uliona jinsi Yehova
Mungu wako alivyokuchukua[m]
kama vile mtu anavyomchu-
kua mwana wake, katika njia
yote mliyoitembea mpaka mli-
pokuja hapa.'[n] **32** Lakini ija-
pokuwa mlikuwa na neno hilo
ninyi hamkuwa na imani ka-
tika Yehova Mungu wenu,[o]
33 aliyekuwa akienda mbele
yenu njiani ili kupeleleza maha-
li kwa ajili yenu ili mpige ka-
mbi,[p] kwa moto wakati wa usi-
ku ili mwione njia mnayopaswa
kuitembea na kwa wingu waka-
ti wa mchana.[q]
34 "Wakati wote huo Yeho-
va alisikia sauti ya maneno
yenu. Basi akakasirika, akaa-
pa,[r] na kusema, **35** 'Hakuna
hata mmoja kati ya watu hawa
wa kizazi hiki kiovu atakayei-
ona ile nchi nzuri niliyoapa ya
kwamba nitawapa baba zenu,[s]
36 isipokuwa Kalebu mwana

SURA 1

a Hes 10:12
Kum 8:15
Yer 2:6
b Mwa 15:16
Hes 13:29
c Hes 13:26
Hes 32:8
d Kum 1:7
e Kum 1:8
Kum 31:6
f Kut 23:27
g Hes 14:9
Yos 1:9
Zb 27:1
Isa 41:10
Ebr 13:6
h Hes 13:2
i Hes 13:3
j Hes 13:17
k Hes 13:24
l Hes 13:23
Hes 13:26
m Hes 13:27
n Ebr 10:38

Safu ya 2

a Hes 14:1
Hes 14:4
Zb 106:24
b Met 19:3
c Kut 3:8
Eze 20:6
d Hes 14:3
e Hes 32:9
Kum 20:8
Yos 14:8
f Hes 13:33
Kum 2:10
g Hes 13:28
Kum 9:1
h Hes 13:22
Yos 11:21
i Hes 14:9
j Kut 14:14
Kum 20:4
Yos 10:42
2Nya 14:11
Zb 46:11
k Hes 14:22
Zb 78:12
Zb 105:27
l Zb 78:15
m Kut 19:4
Kum 32:11
n Zb 77:20
o Zb 78:22
Zb 106:24
Ebr 3:16
Ebr 3:19
Yud 5
p Hes 10:33
q Kut 13:21
Kut 40:36
Hes 10:34
Ne 9:12
Zb 78:14
Zb 105:39
r Hes 14:28
Hes 14:35
Hes 32:10
Kum 2:14
Zb 95:11
Ebr 3:11
s Hes 14:29
Mdo 13:18
1Ko 10:5
Ebr 3:17

wa Yefune.[a] Yeye ataiona, nami
nitampa yeye na wanawe nchi
ile aliyoikanyaga, kwa sababu
amemfuata Yehova kikamili.[b]
37 (Hata mimi Yehova alini-
kasirikia kwa sababu yenu,
na kusema, 'Wewe pia hutai-
ngia humo.[c] **38** Yoshua mwa-
na wa Nuni, anayesimama mbe-
le yako, ndiye atakayeingia
humo.'[d] Yeye amempa nguvu,[e]
kwa sababu atawafanya Isra-
eli wairithi.) **39** Nao watoto
wenu ambao mlisema hivi juu
yao: "Watakuwa nyara!"[f] na
wana wenu ambao leo hawajui
jema wala baya, hao wataingia
humo, nami nitawapa hiyo, nao
wataimiliki. **40** Nanyi wenye-
we, badilini njia mnayoelekea,
mtoke nyikani kupitia njia ya
Bahari Nyekundu.'[g]

41 "Ndipo mlipojibu na kuni-
ambia, 'Tumemtendea dhambi
Yehova.[h] Sisi—sisi tutapanda
na kupigana kulingana na yote
ambayo Yehova Mungu wetu
ametuamuru!' Basi mkajifu-
nga, kila mmoja, silaha zake za
vita nanyi mkaliona kuwa ja-
mbo rahisi kupanda mlimani.[i]
42 Lakini Yehova akaniambia,
'Waambie: "Msipande kwenda
kupigana, kwa sababu mimi
simo katikati yenu;[j] msije mka-
shindwa mbele ya adui zenu."'[k]
43 Basi nikasema nanyi, nanyi
hamkusikiliza bali mkaanza
kujiendesha kwa kumwasi[l] Ye-
hova na kuwaka hasira, nanyi
mkajaribu kwenda juu mlima-
ni.[m] **44** Ndipo Waamori wa-
liokuwa wakikaa katika mli-
ma huo wakatoka ili kukutana
nanyi nao wakawafuatilia ni-
nyi,[n] kama vile nyuki wana-
vyofanya, na kuwatawanya ni-
nyi huko Seiri mpaka Horma.[o]
45 Baada ya jambo hilo mka-

SURA 1

a Hes 14:30
b Hes 14:24
Yos 14:9
c Hes 20:12
Hes 27:13
Kum 3:26
Zb 106:32
d Kut 33:11
Hes 11:28
Hes 14:38
e Hes 27:18
Kum 31:7
Yos 1:6
f Hes 14:3
Hes 14:31
g Hes 14:25
h Hes 14:39
i Hes 14:40
j Law 26:17
Hes 14:42
k Hes 14:43
l Hes 14:41
Isa 63:10
Yer 11:8
Mdo 7:51
m Hes 14:44
n Kum 28:25
Kum 32:30
o Hes 14:45

Safu ya 2

a Zb 78:34
Met 28:9
b Zb 66:18
c Hes 13:25

SURA 2

d Hes 14:25
Kum 1:40
e Kum 2:7
f Mwa 36:8
Hes 20:14
Kum 23:7
g Mwa 27:40
Mwa 36:10
h Mwa 27:39
Mwa 36:9
Kum 2:8
i Kut 15:15
Kut 23:27
Kum 2:25
j Mwa 32:3
Mwa 36:8
Kum 32:8
Yos 24:4
2Nya 20:10
Mdo 17:26
k Hes 20:19
l Mwa 12:2
Met 10:22
m Kum 8:2
Kum 29:5
Zb 95:10
Mdo 13:18
n Ne 9:21
Zb 23:1
Zb 34:9
Zb 34:10
Zb 37:25
Flp 4:19
o Hes 20:20
Hes 20:21
Hes 21:4
Amu 11:18
p Kum 11:30
q 2Nya 8:17
r Hes 21:13
Amu 11:17
2Nya 20:10

rudi na kuanza kulia mbele za
Yehova, lakini Yehova hakui-
sikiliza sauti yenu,[a] wala haku-
wategea ninyi sikio.[b] **46** Basi
mkaendelea kukaa kule Kade-
shi siku nyingi, siku nyingi ka-
diri mlivyokaa huko.[c]

2 "Kisha tukageuka na kuo-
ndoka kuelekea nyikani ku-
pitia njia ya Bahari Nyekundu,
kama vile Yehova alivyokuwa
amesema nami;[d] nasi tukauzu-
nguka Mlima Seiri kwa siku
nyingi. **2** Mwishowe Yehova
akaniambia hivi, **3** 'Mmeuzu-
nguka mlima huu muda mrefu
vya kutosha.[e] Geukeni mwele-
kee kaskazini. **4** Nawe uwaa-
muru watu, na kusema: "Mna-
pita kando ya mpaka wa ndu-
gu zenu,[f] wana wa Esau,[g]
ambao wanakaa Seiri,[h] nao wa-
taogopa kwa sababu yenu,[i]
nanyi lazima muwe waangali-
fu sana. **5** Msigombane nao,
kwa sababu sitawapa ninyi se-
hemu ya nchi yao hata upana
wa wayo wa mguu; kwa saba-
bu nimempa Esau Mlima Sei-
ri uwe miliki yake.[j] **6** Chaku-
la mtakachonunua kutoka
kwao kwa pesa, mtakula; na
pia maji mtakayonunua kutoka
kwao kwa pesa, mtakunywa.[k]
7 Kwa maana Yehova Mungu
wako amekubariki wewe kati-
ka kila tendo la mkono wako.[l]
Anajua vema juu ya kutembea
kwako katika nyika hii kuu.
Miaka hii 40[m] Yehova Mungu
wako amekuwa pamoja nawe.
Hukukosa kitu chochote."'[n]
8 Basi tukapita mbali na ndu-
gu zetu, wana wa Esau,[o] wana-
okaa Seiri, kutoka njia ya Ara-
ba,[p] kutoka Elathi na kutoka
ESION-GEBERI.[q]

"Kisha tukageuka na kupi-
tia njia ya nyika ya Moabu.[r]

9 Ndipo Yehova akaniambia,
'Usimsumbue Moabu wala ku-
pigana vita naye, kwa sababu
sitakupa wewe sehemu yoyote
ya nchi yake iwe miliki yako,
kwa maana wana wa Loti[a] ni-
mewapa Ari[b] iwe miliki yao.
10 (Waemi[c] walikaa humo nya-
kati za kale, watu wakubwa na
wengi sana na warefu kama
Waanaki.[d] **11** Nao Warefai-
mu,[e] wao pia walionwa kama
Waanaki,[f] na Wamoabu waliku-
wa wakiwaita Waemi. **12** Nao
Wahori[g] walikaa Seiri nyakati
za kale, na wana wa Esau[h] wa-
kawafukuza na kuwaangami-
za kutoka mbele yao, wakakaa
mahali pao,[i] kama vile Israeli
atakavyoitendea nchi iliyo mi-
liki yake, ambayo hakika Yeho-
va atawapa.) **13** Wakati huu
ondokeni mshike njia na kuvu-
ka bonde la mto la Zeredi.' Basi
tukavuka bonde la mto la Zere-
di.[j] **14** Na siku tulizotembea
kutoka Kadesh-barnea mpaka
tulipovuka bonde la mto la Ze-
redi zilikuwa miaka 38, mpaka
kizazi chote cha wanaume wa
vita kilipokuwa kimefikia mwi-
sho wake kutoka katika kambi,
kama vile Yehova alivyokuwa
amewaapia.[k] **15** Na mkono[l]
wa Yehova pia ulikuwa juu yao
ili kuwafadhaisha kutoka ka-
tika kambi, mpaka walipofikia
mwisho wao.[m]

16 "Na ikawa kwamba mara
tu wanaume hao wa vita
walipokwisha kufa wote kuto-
ka kati ya watu,[n] **17** Yehova
akazidi kusema nami, na ku-
niambia hivi, **18** 'Leo utapi-
ta karibu na eneo la Moabu,
yaani, Ari,[o] **19** nawe utakari-
bia mbele ya wana wa Amo-
ni. Usiwasumbue wala usigo-
mbane nao, kwa sababu sita-
kupa sehemu yoyote ya nchi
ya wana wa Amoni iwe miliki
yako, kwa maana nimewapa
wana wa Loti iwe miliki yao.[a]
20 Hiyo pia ilikuwa ikionwa
kuwa nchi ya Warefaimu.[b] (Wa-
refaimu walikaa humo nyakati
za kale, nao Waamoni waliku-
wa wakiwaita hao Wazamzumi.
21 Walikuwa wakubwa na we-
ngi sana na watu warefu kama
Waanaki;[c] naye Yehova akawa-
angamiza[d] kutoka mbele yao,
ili wapate kuwafukuza na ku-
kaa mahali pao; **22** kama vile
alivyowafanyia wana wa Esau,
wanaokaa Seiri,[e] wakati amba-
po aliwaangamiza Wahori[f] ku-
toka mbele yao, ili wapate ku-
wafukuza na kukaa mahali pao
mpaka leo hii. **23** Nao Waa-
vi,[g] waliokuwa wakikaa katika
makao yaliyoko mpaka Gaza,[h]
Wakaftori,[i] waliotoka Kafto-
ri,[j] wakawaangamiza, ili wapa-
te kukaa mahali pao.)

24 "'Ondokeni, mshike njia
na kuvuka bonde la mto la
Arnoni.[k] Tazama, nimemtia
mkononi mwako Sihoni[l] mfalme
wa Heshboni, yule Mwamori.
Kwa hiyo anza kumiliki nchi
yake, na kupigana vita naye.
25 Leo nitaanza kutia hofu
kwa ajili yako na woga kwa aji-
li yako mbele ya watu chini
ya mbingu zote, ambao watasi-
kia habari juu yako; nao watafa-
dhaika na kuwa na maumivu
kama yale ya kuzaa kwa sababu
yako.'[m]

26 "Ndipo nikatuma waju-
mbe kutoka katika nyika ya
Kedemothi[n] mpaka kwa Siho-
ni[o] mfalme wa Heshboni waki-
wa na maneno ya amani,[p] na
kusema, **27** 'Niruhusu nipite
katika nchi yako. Nitatembea

SURA 2

a Mwa 19:37
b Hes 21:15
Kum 2:18
Isa 15:1
c Mwa 14:5
d Hes 13:33
Yos 14:15
e Mwa 14:5
Kum 3:11
1Nya 20:6
f Hes 13:22
Hes 13:28
Hes 13:33
Kum 1:28
Kum 9:2
g Mwa 14:6
Mwa 36:20
1Nya 1:39
h Mwa 36:10
i Mwa 27:39
Mwa 27:40
j Hes 21:12
k Hes 14:33
Hes 32:11
Kum 1:35
Zb 95:11
Zb 106:26
Eze 20:15
Ebr 3:18
Yud 5
l Ebr 10:31
m 1Ko 10:5
n Hes 26:64
o Hes 21:15
Hes 21:28

Safu ya 2

a Mwa 19:38
Kum 2:9
Amu 11:15
2Nya 20:10
Mdo 17:26
b Mwa 15:20
Kum 3:11
Yos 17:15
c Hes 13:33
Kum 2:10
Kum 9:2
d Kut 15:3
Zb 24:8
e Mwa 36:8
f Mwa 14:6
Mwa 36:20
Kum 2:12
g Yos 13:3
h Mwa 10:19
Yos 11:22
i Mwa 10:14
1Nya 1:12
j Yer 47:4
Amo 9:7
Mdo 27:13
k Hes 21:13
Amu 11:18
l Hes 21:23
Yos 9:10
m Kut 15:14
Kut 23:27
Kum 11:25
Yos 2:9
n Yos 13:18
Yos 21:37
o Hes 21:21
p Kum 20:10

barabarani tu. Sitageuka ku-
ume wala kushoto.[a] **28** Cha-
kula utakachoniuzia kwa pesa,
ndicho nitakachokula; na maji
utakayonipa kwa pesa, ndiyo
nitakayokunywa. Ila tu uni-
ruhusu nipite kwa miguu ya-
ngu,[b] **29** kama vile wana wa
Esau wanaokaa Seiri[c] na Wa-
moabu[d] wanaokaa Ari walivyo-
nifanyia, mpaka nitakapokuwa
nimevuka Yordani na kuingia
nchi ambayo Yehova Mungu
wetu anatupa sisi.'[e] **30** Naye
Sihoni mfalme wa Heshbo-
ni hakuturuhusu tupite kati-
kati yake, kwa sababu Yehova
Mungu wako alikuwa ameiacha
roho yake iwe kaidi[f] na moyo
wake uwe mgumu, ili amtie
mkononi mwako kama ilivyo
leo hii.[g]

31 "Ndipo Yehova akaniam-
bia, 'Tazama, nimeanza ku-
mtia Sihoni na nchi yake mko-
noni mwako. Anza kuimiliki
nchi yake.'[h] **32** Sihoni alipo-
toka nje, yeye na watu wake
wote, ili kukutana nasi vitani
huko Yahazi,[i] **33** ndipo Yeho-
va Mungu wetu alipomtia mko-
noni mwetu,[j] hivi kwamba tu-
kamshinda yeye[k] na wanawe na
watu wake wote. **34** Nasi tu-
kateka majiji yake yote waka-
ti huo na kuangamiza[l] kila jiji,
wanaume na wanawake na wa-
toto wadogo. Hatukuacha
mwokokaji yeyote. **35** Ila wa-
nyama wa kufugwa ndio tuli-
ochukua wawe nyara zetu, pa-
moja na nyara za majiji tuliyo-
kuwa tumeteka.[m] **36** Toka
Aroeri,[n] jiji lililo kando ya uki-
ngo wa bonde la mto la Arno-
ni, na lile jiji lililo katika bonde
la mto, mpaka Gileadi, haku-
kuwa na mji wowote uliokuwa
juu sana kwetu.[o] Yehova Mu-
ngu wetu aliitia yote mkononi
mwetu. **37** Ila wewe hukwe-
nda karibu na nchi ya wana wa
Amoni,[a] ukingo mzima wa bo-
nde la mto la Yaboki,[b] wala ma-
jiji ya eneo lenye milima, wala
kitu chochote ambacho juu
yake Yehova Mungu wetu aliku-
wa ametoa amri.

3 "Kisha tukageuka na ku-
panda kupitia njia ya Ba-
shani. Ndipo Ogu[c] mfalme
wa Bashani akatoka nje, yeye
na watu wake wote, ili kuku-
tana nasi katika pigano huko
Edrei.[d] **2** Basi Yehova aka-
niambia, 'Usimwogope,[e] kwa
maana nitamtia yeye na watu
wake wote na nchi yake mko-
noni mwako; nawe utamtendea
kama vile ulivyomtendea Siho-
ni[f] mfalme wa Waamori, aliye-
kuwa akikaa kule Heshboni.'
3 Basi Yehova Mungu wetu
akamtia mkononi mwetu pia
Ogu mfalme wa Bashani pa-
moja na watu wake wote, nasi
tukaendelea kumpiga mpaka
akawa hana mwokokaji aliye-
baki.[g] **4** Nasi tukateka maji-
ji yake yote wakati huo. Haku-
kuwa na mji wowote ambao ha-
tukuuchukua kutoka kwao,
majiji 60,[h] eneo lote la Argobu,[i]
ufalme wa Ogu katika Basha-
ni.[j] **5** Majiji yote hayo yali-
kuwa yametiwa ngome ya uku-
ta mrefu, milango na mapingo,
mbali na miji mingi sana ya
mashambani. **6** Hata hivyo,
tuliwaangamiza,[k] kama vile
tulivyomtendea Sihoni mfa-
lme wa Heshboni, kwa kua-
ngamiza kila jiji, mwanamume,
mwanamke na watoto wadogo.[l]
7 Na wanyama wote wa kufu-
gwa na nyara za majiji tuka-
chukua kuwa nyara kwa ajili
yetu wenyewe.[m]

SURA 2
a Hes 21:22
Amu 11:19
b Hes 20:19
c Kum 2:8
d Kum 2:9
Kum 2:18
e Kum 9:5
Yos 1:11
f Ayu 34:11
Ro 9:18
g Hes 21:25
Zb 135:10
Zb 136:18
h Hes 32:33
Zb 135:12
i Hes 21:23
Amu 11:20
j Kum 20:13
Ne 9:22
Zb 135:11
Zb 136:18
k Hes 21:24
Kum 29:7
l Law 27:28
Hes 31:17
Kum 20:16
Kum 20:17
m Yos 8:27
n Kum 3:12
Kum 4:48
Yos 13:9
o Yos 1:5
Zb 44:3

Safu ya 2
a Kum 3:16
Amu 11:15
b Hes 21:24
Yos 12:2

SURA 3
c Hes 21:33
Kum 29:7
Yos 9:10
Ne 9:22
d Yos 12:4
Yos 13:12
e Hes 14:9
Hes 21:34
Kum 20:3
f Hes 21:24
g Hes 21:35
Yos 13:12
h Hes 32:33
Yos 13:30
i 1Fa 4:13
j Kum 29:8
k Law 27:29
l Law 18:25
Kum 2:34
Eze 9:6
m Kum 2:35
Yos 8:27

8 "Nasi tukaendelea kuchukua wakati huo ile nchi kutoka mkononi mwa wale wafalme wawili wa Waamori[a] waliokuwa katika eneo la Yordani, kutoka katika bonde la mto la Arnoni[b] mpaka Mlima Hermoni;[c] **9** (Wasidoni walikuwa wakiuita Hermoni Sirioni,[d] nao Waamori walikuwa wakiuita Seniri,)[e] **10** majiji yote ya nchi tambarare ya juu na Gileadi yote na Bashani yote mpaka Saleka[f] na Edrei,[g] majiji ya ufalme wa Ogu katika Bashani. **11** Kwa maana Ogu mfalme wa Bashani ndiye tu aliyebaki kati ya mabaki ya Warefaimu.[h] Tazama! Sanduku lake lilikuwa sanduku la chuma. Je, haliko kule Raba[i] kwa wana wa Amoni? Urefu wake ni mikono tisa, na upana wake ni mikono minne, kwa mkono wa mwanadamu. **12** Nasi tukaitwaa nchi hii wakati huo; kutoka Aroeri,[j] kando ya bonde la Arnoni, na nusu ya eneo lenye milima la Gileadi, na majiji yake nimewapa Warubeni na Wagadi.[k] **13** Na ile Gileadi[l] nyingine na Bashani[m] yote ya ufalme wa Ogu nimewapa nusu ya kabila la Manase. Eneo lote la Argobu[n] la Bashani yote, je, haliitwi nchi ya Warefaimu?[o]

14 "Yairi[p] mwana wa Manase alichukua eneo lote la Argobu[q] hadi mpaka wa Wageshuri[r] na Wamaakathi,[s] naye akaviita vijiji hivyo vya Bashani kwa jina lake mwenyewe, Hawoth-yairi,[t] mpaka leo hii. **15** Na Makiri[u] nimempa Gileadi.[v] **16** Na Warubeni[w] na Wagadi nimewapa kutoka Gileadi[x] hadi kwenye bonde la mto la Arnoni, mpaka ukiwa ni katikati ya lile bonde la mto, hadi Yaboki, lile bonde la mto lililo mpakani mwa wana wa Amoni;[a] **17** na Araba na Yordani na ule mpaka, kutoka Kinerethi[b] hadi bahari ya Araba, Bahari ya Chumvi,[c] chini ya mteremko wa Pisga[d] kuelekea mashariki.

18 "Basi nikawaamuru ninyi wakati huo, na kusema, 'Yehova Mungu wenu amewapa nchi hii mpate kuimiliki. Mtavuka, mkiwa tayari na silaha, mbele ya ndugu zenu, wana wa Israeli, wanaume wote mashujaa.[e] **19** Ila wake zenu na watoto wenu na mifugo yenu (najua kwamba mna kiasi kikubwa cha mifugo) wataendelea kukaa katika majiji yenu ambayo nimewapa ninyi,[f] **20** mpaka Yehova atakapowapa ndugu zenu pumziko, kama ninyi, nao pia wawe wamemiliki nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa ng'ambo ya Yordani; ndipo mtakaporudi, kila mmoja kwenda kwenye miliki yake ambayo nimewapa ninyi.'[g]

21 "Nami nikamwamuru Yoshua[h] wakati huo, na kusema, 'Macho yako yanaona yote ambayo Yehova Mungu wako amewafanyia wafalme hao wawili. Hivyo ndivyo Yehova atakavyozifanyia falme zote ambazo mnavuka kuziendea huko.[i] **22** Msiwaogope, kwa maana Yehova Mungu wenu Ndiye anayewapigania ninyi.'[j]

23 "Nami nikamwomba Yehova kibali wakati huo, na kusema, **24** 'Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, wewe mwenyewe umeanza kumfanya mtumishi wako aone ukuu[k] wako na mkono wako wenye nguvu,[l] kwa maana ni nani aliye mungu mbinguni au

SURA 3

a Hes 32:33
b Yos 12:2
Yos 13:9
c Yos 11:3
Wim 4:8
d Zb 29:6
e 1Nya 5:23
Eze 27:5
f Yos 12:5
Yos 13:11
g Hes 21:33
Yos 13:12
h Mwa 14:5
i 2Sa 12:26
Yer 49:2
j Hes 32:34
Kum 4:48
Yos 12:2
k Hes 32:33
l Mwa 31:21
Hes 32:39
Yos 13:31
Amu 10:4
m Yos 13:30
1Nya 5:23
n 1Fa 4:13
o Mwa 15:20
p 1Nya 2:22
q Kum 3:4
r Yos 13:13
2Sa 3:3
s Yos 12:5
t Hes 32:41
u Mwa 50:23
Yos 17:1
v Hes 32:39
w Hes 32:33
x Kum 3:8
Yos 22:9

Safu ya 2

a Hes 21:24
Yos 12:2
b Hes 34:11
c Mwa 14:3
Hes 34:12
Yos 12:3
d Kum 34:1
e Hes 32:20
f Yos 1:14
g Yos 1:15
Yos 22:4
Yos 22:8
h Hes 11:28
Hes 14:30
Hes 27:18
i Yos 10:25
j Kut 14:14
Kut 15:3
Hes 21:34
Kum 1:30
Kum 20:4
Yos 10:42
k Kut 34:6
Kum 11:2
Zb 145:3
Yer 32:18
l Kut 15:16
Zb 44:3

duniani ambaye hutenda matendo kama yako na utendaji wenye nguvu kama wako?[a]
25 Acha nivuke, tafadhali, niione hiyo nchi nzuri[b] iliyo
ng'ambo ya Yordani, eneo hilo
zuri lenye milima[c] na Lebanoni.'[d] **26** Na Yehova akaendelea kuwa na ghadhabu juu yangu kwa sababu yenu[e] wala hakunisikiliza; lakini Yehova aliniambia, 'Imetosha! Usiseme nami tena kamwe juu ya jambo hili. **27** Panda juu ya Pisga,[f] uinue macho yako kuelekea magharibi na kaskazini na kusini na mashariki, uone kwa macho yako, kwa maana wewe hutavuka huu mto Yordani.[g]
28 Nawe umpe Yoshua utume[h]
na kumtia moyo na kumwimarisha, kwa maana yeye ndiye atakayevuka[i] mbele ya watu
hawa naye ndiye atakayewafanya warithi nchi utakayoiona.'[j]
29 Wakati wote huo tulikuwa tukikaa katika lile bonde mbele ya Beth-peori.[k]

4 "Na sasa, Ee Israeli, sikilizeni masharti na maamuzi ya hukumu ninayowafundisha ninyi kufanya, ili mpate kuishi[l] na kwa kweli mpate kuingia na kuimiliki nchi ambayo Yehova Mungu wa mababu zenu anawapa ninyi. **2** Nanyi msiongeze kwenye neno ninalowaamuru ninyi, wala msiondoe lolote kutoka katika hilo,[m] ili mzishike amri za Yehova Mungu wenu ninazowaamuru ninyi.

3 "Macho yenu wenyewe ndiyo yaliyoona mambo ambayo Yehova alifanya katika kile kisa cha Baali wa Peori,[n] kwamba kila mtu aliyemfuata Baali wa Peori ndiye ambaye Yehova Mungu wako aliangamiza kutoka katikati yako.[o] **4** Lakini ninyi mnaoshikamana[a] na Yehova Mungu wenu, nyote mko hai leo. **5** Tazama! nimewafundisha masharti[b] na maamuzi ya hukumu,[c] kama vile ambavyo Yehova Mungu wangu ameniamuru mimi, ili ninyi mfanye hivyo katikati ya nchi ambayo mnaenda kuimiliki. **6** Nanyi mtazishika na kuzifanya, kwa sababu hiyo ni hekima[d] kwenu na uelewaji[e] kwenu mbele ya macho ya vikundi vya watu watakaosikia juu ya masharti yote haya, nao watasema, 'Taifa hili kubwa bila shaka ni watu wenye hekima na wenye uelewaji.'[f]
7 Kwa maana ni taifa[g] gani kubwa ambalo lina miungu iliyo karibu nalo kama Yehova Mungu wetu alivyo tunapomwitia nyakati zote?[h] **8** Na kuna taifa gani kubwa lenye masharti na maamuzi ya hukumu ya uadilifu kama sheria yote hii ninayoweka mbele yenu leo?[i]

9 "Ila jiangalie na kuitunza vema nafsi yako,[j] ili usisahau mambo ambayo macho yako yameona,[k] nayo yasiondoke moyoni mwako siku zote za maisha yako;[l] nawe utawajulisha mambo hayo wana wako na wajukuu wako,[m] **10** siku ambayo ulisimama mbele za Yehova Mungu wako katika Horebu,[n] wakati ambapo Yehova aliniambia, 'Kutanisha watu pamoja kwangu ili niwafanye wasikie maneno yangu,[o] ili wapate kujifunza kuniogopa[p] mimi siku zote walizo hai juu ya nchi na ili wawafundishe wana wao.'[q]

11 "Kwa hiyo mkaja karibu na kusimama chini ya mlima,

SURA 3
a Kut 15:11; 2Sa 7:22; 1Fa 8:23; Zb 71:19; Zb 86:8; Yer 10:6; Yer 49:19
b Kut 3:8; Kum 4:22; Kum 11:12; Eze 20:6
c Kum 1:7
d Yos 13:5; 1Fa 9:19
e Hes 20:12; Hes 27:14; Kum 31:2; Zb 106:32
f Hes 21:20; Hes 27:12; Kum 34:1
g Kum 34:4
h Hes 27:19; Kum 1:38; Kum 31:7
i Yos 1:2; Mdo 7:45
j Yos 3:7
k Kum 4:46; Kum 34:6; Yos 13:20

SURA 4
l Law 18:5; Eze 20:11; Ro 10:5
m Kum 12:32; Yos 1:7; Met 30:6; Ufu 22:18
n Hes 25:3; Yos 22:17; Zb 106:28; Ho 9:10; 1Ko 10:7
o Hes 25:5; Hes 25:9; 1Ko 10:8

Safu ya 2
a Kum 10:20; Kum 13:4; Yos 22:5
b Law 10:11; Law 26:46; Hes 30:16
c Law 25:18; Hes 36:13; Kum 6:1
d 1Fa 2:3; Zb 19:7; Zb 107:43; Zb 111:10; Zb 119:98; Met 10:8; Yer 8:9
e Zb 119:100; Met 4:7
f 1Fa 4:34; 1Fa 10:7; Da 1:20
g 2Sa 7:23
h Kut 25:8; Law 26:12; Kum 5:26; Zb 46:1; Zb 145:18
i Zb 78:5; Zb 147:19
j Met 4:23; Met 19:16
k Met 4:21
l Met 3:1; Met 7:1; Ebr 2:1

m Mwa 18:19; Kum 6:7; Zb 78:5; n Kum 5:2; o Kut 19:9; Ebr 12:25; p Kut 20:20; Kum 5:29; 1Sa 12:24; Lu 1:50; q Met 22:6; Efe 6:4.

nao mlima ulikuwa ukiwaka
moto mpaka katikati ya mbi-
ngu; kulikuwa na giza, wingu
na weusi mzito.[a] **12** Naye Ye-
hova akaanza kusema nanyi
kutoka katikati ya moto.[b] Sa-
uti ya maneno ndiyo mliyoku-
wa mkiisikia, bali hamkuwa
mkiona umbo[c] lolote—mlisikia
sauti tu.[d] **13** Naye akawajuli-
sha ninyi agano[e] lake, alilowaa-
muru mtende—yale Maneno
Kumi,[f] kisha akayaandika juu
ya mabamba mawili ya mawe.[g]
14 Na Yehova aliniamuru mimi
wakati huo niwafundishe ma-
sharti na maamuzi ya huku-
mu, ili ninyi myatende katika
nchi ambayo mnavuka ili kui-
miliki.[h]

15 "Nanyi mjiangalie vema
nafsi zenu,[i] kwa sababu ha-
mkuona umbo[j] lolote katika
siku ambayo Yehova alise-
ma nanyi katika Horebu ku-
toka katikati ya moto, **16** ili
msitende kwa uharibifu[k] wala
msijifanyie wenyewe sanamu
ya kuchongwa, umbo la mfano
wowote, mfano wa mwanamu-
me au mwanamke,[l] **17** mfano
wa mnyama yeyote aliye du-
niani,[m] mfano wa ndege ye-
yote mwenye mabawa ambaye
huruka mbinguni,[n] **18** mfa-
no wa kitu chochote kinacho-
tembea kwenye nchi, mfano
wa samaki[o] yeyote aliye kati-
ka maji chini ya dunia;
19 wala usije ukayainua macho
yako mbinguni na kuona jua
na mwezi na nyota, jeshi lote
la mbinguni, nawe upate kusha-
wishiwa na kuviinamia na ku-
vitumikia,[p] vile ambavyo Yeho-
va Mungu wako amegawia vi-
kundi vyote vya watu chini ya
mbingu nzima.[q] **20** Lakini ni-
nyi ndio watu ambao Yehova
alichukua apate kuwatoa nje
ya tanuru ya chuma,[a] toka nje
ya Misri, ili muwe watu wa mali
ya kibinafsi kwake[b] kama ilivyo
leo hii.

21 "Na Yehova akaniwakia
hasira kwa sababu yenu,[c] hivi
kwamba akaapa kwamba sita-
vuka Yordani wala kuingia ka-
tika ile nchi nzuri ambayo Ye-
hova Mungu wako anakupa iwe
urithi wako.[d] **22** Kwa maana
ninakufa katika nchi hii.[e] Sivu-
ki Yordani, lakini ninyi mnavu-
ka, nanyi mtaimiliki nchi hiyo
nzuri. **23** Jiangalieni msije
mkasahau agano la Yehova Mu-
ngu wenu ambalo alifanya pa-
moja nanyi[f] na msijifanyie sa-
namu ya kuchongwa, umbo
la kitu chochote ambacho
juu yake Yehova Mungu wako
amekuamuru.[g] **24** Kwa maa-
na Yehova Mungu wako ni moto
unaoteketeza,[h] Mungu anaye-
taka watu wajitoe kikamili.[i]

25 "Ikiwa utakuwa baba ya
wana na wajukuu nanyi mme-
kaa muda mrefu katika nchi na
kutenda kwa uharibifu[j] na ku-
fanya sanamu ya kuchongwa,[k]
umbo la kitu chochote, na ku-
fanya uovu machoni pa Yehova
Mungu[l] wako na kumtia uchu-
ngu, **26** leo nachukua mbi-
ngu na dunia ili ziwe mashahidi
dhidi yenu,[m] ya kwamba haki-
ka mtaangamia haraka kutoka
katika nchi ambayo mnavuka
Yordani ili mwimiliki. Hamta-
refusha siku zenu juu yake,
kwa sababu hakika mtaanga-
mizwa.[n] **27** Na Yehova ata-
watawanya ninyi katikati ya
watu,[o] nanyi mtabaki hesabu
chache[p] katikati ya mataifa
ambayo Yehova atayafukuzia

SURA 4
a Kut 19:18
Kum 5:23
Ebr 12:18
b Kum 9:10
Kum 10:4
c Kum 4:15
Isa 40:18
Yoh 1:18
Yoh 4:24
d Kut 20:22
Ebr 12:19
e Kut 19:5
Kum 5:2
Kum 9:9
Ebr 9:20
f Kut 20:1
Kut 34:28
Kum 10:4
g Kut 24:12
Kut 31:18
Kut 32:19
Kut 34:1
h Zb 105:44
i Kum 6:24
Yos 23:11
j Kum 4:12
k Kut 32:7
l Kut 20:4
Kum 27:15
Isa 40:18
Mdo 17:29
1Ko 10:14
m Ro 1:23
n Kum 5:8
o 1Sa 5:4
p Kum 17:3
2Fa 17:16
Yer 8:2
Eze 8:16
Sef 1:5
Mdo 7:43
q Zb 136:7
Yer 31:35

Safu ya 2
a 1Fa 8:51
Yer 11:4
b Kut 19:5
Kum 9:26
1Fa 8:53
Zb 135:4
c Hes 20:12
Kum 3:26
d Kum 31:2
Zb 106:32
e Kum 3:27
f Kut 19:5
Kut 24:3
g Kut 20:4
Kum 4:16
1Ko 10:14
h Kut 24:17
Kum 9:3
Ebr 12:29
i Kut 20:5
Kut 34:14
Hes 25:11
Yos 24:19
Nah 1:2
Lu 10:27
j Kut 32:7
Kum 4:16
k Amu 18:30
2Fa 17:16
2Fa 21:7
Isa 42:8
l 2Fa 17:17
m Kum 30:19
Kum 31:28
Isa 1:2
n Law 18:28
Law 26:32
Kum 29:28
Yos 23:16
Isa 24:1

o Kum 28:64; Ne 1:8; Eze 12:15; p Kum 28:62.

mbali. **28** Na huko mtalazimika kuitumikia miungu mingine,[a] kazi ya mikono ya mwanadamu, miti na mawe,[b] ambayo haiwezi kuona wala kusikia wala kula wala kunusa.[c]

29 "Mkimtafuta Yehova Mungu wenu mkiwa huko, hakika mtampata pia,[d] kwa sababu utauliza kumhusu kwa moyo wako wote na kwa nafsi yako yote.[e] **30** Utakapokuwa katika dhiki kali na maneno yote haya yawe yamekupata mwishoni mwa siku hizo, basi utarudi kwa Yehova Mungu[f] wako na kuisikiliza sauti yake.[g] **31** Kwa maana Yehova Mungu wako ni Mungu mwenye rehema.[h] Hatakutupa wala kukuharibu wala kulisahau agano[i] la mababu zako ambalo aliwaapia.

32 "Sasa uliza, tafadhali, juu ya siku za zamani[j] zilizokuwapo kabla yako, kutoka siku ambayo Mungu alimuumba mwanadamu duniani[k] na kutoka mwisho mmoja wa mbingu mpaka mwisho mwingine wa mbingu, Je, jambo lolote kubwa kama hili lilitokezwa au jambo lolote kama hili lilisikiwa?[l] **33** Je, kundi lingine lolote la watu limesikia sauti ya Mungu ikisema kutoka katikati ya moto jinsi ambavyo wewe mwenyewe umeisikia, nao wakaendelea kuishi?[m] **34** Au je, Mungu alijaribu kuja kuchukua taifa kwa ajili yake mwenyewe kutoka kati ya taifa lingine kwa uthibitisho,[n] kwa ishara[o] na kwa miujiza[p] na kwa vita[q] na kwa mkono wenye nguvu[r] na kwa mkono ulionyooshwa[s] na kwa woga mkuu[t] kama yote ambayo Yehova Mungu wenu amewafanyia ninyi katika Misri mbele ya macho yako? **35** Wewe—wewe umeonyeshwa, ili upate kujua kwamba Yehova ndiye Mungu wa kweli;[a] hakuna mwingine isipokuwa yeye.[b] **36** Kutoka mbinguni alikufanya usikie sauti yake ili kukurekebisha; na duniani alikufanya uone moto wake mkuu, nayo maneno yake uliyasikia kutoka katikati ya moto huo.[c]

37 "Na hata hivyo unaendelea kuishi, kwa sababu aliwapenda mababu zako hivi kwamba akachagua uzao wao baada yao[d] na kukuleta kutoka Misri mbele za macho yake kwa nguvu zake kuu,[e] **38** ili kuyafukuzia mbali mataifa makubwa zaidi na yenye nguvu zaidi kuliko wewe kutoka mbele yako, ili akulete ndani, akupe nchi yao iwe urithi kama ilivyo leo hii.[f] **39** Nawe unajua vema leo, nawe ukumbuke moyoni mwako kwamba Yehova ndiye Mungu wa kweli mbinguni juu na duniani chini.[g] Hakuna mwingine.[h] **40** Nawe lazima uyashike masharti yake[i] na amri zake ninazokuamuru leo, ili mambo yakuendee vema wewe[j] na wana wako baada yako, na ili urefushe siku zako juu ya nchi ambayo Yehova Mungu wako anakupa,[k] sikuzote."

41 Wakati huo Musa akatenga majiji matatu upande wa Yordani kuelekea mashariki,[l] **42** ili akimbilie humo yule atakayemuua mwenzake bila kujua,[m] ikiwa hakuwa akimchukia hapo kwanza;[n] naye atakimbilia moja la majiji hayo naye ataishi,[o] **43** yaani, Beseri[p] katika nyika kwenye nchi tambarare ya juu kwa ajili ya

SURA 4
a Yer 16:13; Eze 20:39
b Kum 28:36; Eze 20:32
c Zb 115:5; Zb 135:16; Isa 44:9; Ufu 9:20
d Kum 30:10; 2Nya 15:4; 2Nya 15:15
e Kum 30:2; 1Fa 8:48; Yer 29:13; Yoe 2:12
f Kum 30:10; 2Nya 33:13; Ne 1:9
g Yer 7:23
h Kut 34:6; Kum 30:3; 2Nya 30:9; Ne 9:31; Zb 86:15; Isa 54:7; Isa 55:7; 2Ko 1:3
i Law 26:42; Zb 105:8; Lu 1:72
j Zb 44:1
k Mwa 2:7
l Kut 15:11
m Kum 5:26
n Kum 7:19
o Kut 7:3
p Zb 105:27
q Kut 15:3
r Kut 13:3; Kum 6:21
s Kut 6:6
t Kum 26:8; Zb 78:49; Yer 32:21

Safu ya 2
a Kut 3:14; Kut 6:7; 1Fa 18:37; 2Fa 19:19; Zb 83:18
b Kut 15:11; Kum 32:39; 1Sa 2:2; Isa 45:18; Mk 12:32
c Kut 19:18; Kut 20:22; Kum 4:12; Kum 4:15; Kum 4:33; Ne 9:13; Ebr 12:18; Ebr 12:25
d Kum 10:15; Zb 105:6
e Kut 13:14; Yer 32:21
f Kut 23:28; Kum 7:1; Kum 9:1; Yos 3:10; Zb 44:2
g Yos 2:11; 2Nya 20:6; Zb 135:6; Da 4:35
h Kum 4:35; Isa 44:6
i Kum 4:5
j Kum 5:16
k Mwa 48:4
l Hes 35:14
m Hes 35:11; Hes 35:22

n Kum 19:4; o Hes 35:25; p Yos 21:36.

Warubeni, na Ramothi[a] katika
Gileadi kwa ajili ya Wagadi, na
Golani[b] katika Bashani kwa aji-
li ya Wamanase.[c]
44 Sasa hii ndiyo sheria[d]
ambayo Musa aliweka mbele
ya wana wa Israeli. **45** Huu
ndio ushuhuda[e] na masharti[f]
na maamuzi ya hukumu[g] amba-
yo Musa aliwaambia wana wa
Israeli walipokuwa wakitoka
Misri, **46** katika eneo la Yor-
dani katika bonde mbele ya
Beth-peori,[h] katika nchi ya Si-
honi mfalme wa Waamori, ali-
yekuwa akikaa Heshboni,[i]
ambaye Musa na wana wa Isra-
eli walimshinda walipokuwa
wakitoka Misri.[j] **47** Nao wa-
kaimiliki nchi yake na nchi
ya Ogu[k] mfalme wa Bashani,
wale wafalme wawili wa Wa-
amori waliokuwa katika eneo
la Yordani kuelekea mashariki,
48 kutoka Aroeri,[l] jiji lililoko
ukingoni mwa bonde la mto la
Arnoni, mpaka Mlima Sioni, ya-
ani, Hermoni,[m] **49** na Araba[n]
yote katika eneo la Yordani ku-
elekea mashariki, na mpaka
bahari ya Araba[o] chini ya mite-
remko ya Pisga.[p]

5 Na Musa akaita Israeli[q]
wote na kuwaambia: "Si-
kia, Ee Israeli, masharti na
maamuzi ya hukumu[r] amba-
yo ninasema masikioni mwe-
nu leo, nanyi mjifunze hayo na
kuwa waangalifu kuyatenda.[s]
2 Yehova Mungu wetu alifa-
nya agano pamoja nasi kati-
ka Horebu.[t] **3** Yehova haku-
fanya agano hili pamoja na ma-
babu zetu, bali pamoja nasi, sisi
sote tulio hai hapa leo. **4** Uso
kwa uso Yehova alisema pamo-
ja nanyi katika mlima kutoka
katikati ya moto.[u] **5** Mimi ni-
likuwa nimesimama katikati ya

SURA 4

a Yos 21:38
b Yos 21:27
c Yos 20:8
d Kum 17:18
Kum 27:3
Mal 4:4
Yoh 1:17
Ga 3:24
e Kum 6:17
1Fa 2:3
f Law 26:46
Kum 4:1
g Law 18:5
Kum 4:5
Ne 9:13
Zb 119:164
Eze 20:11
h Kum 1:5
Kum 3:29
i Hes 21:26
j Hes 21:24
k Hes 21:33
Kum 3:4
Kum 29:7
l Kum 2:36
Kum 3:12
m Kum 3:9
Yos 11:3
n Kum 1:7
Yos 12:3
o Mwa 14:3
Kum 3:17
p Kum 34:1

SURA 5

q Kum 1:1
Kum 29:10
r Kum 4:5
s Kum 4:1
t Kut 19:5
Kum 4:23
Ebr 9:19
u Kut 19:9
Kut 19:18
Kut 20:22
Kum 4:33
Mdo 7:38

Safu ya 2

a Kut 20:19
Kum 34:10
Ga 3:19
b Kut 19:16
c Zb 81:10
Ho 13:4
d Kut 13:3
Kut 20:2
e Kut 20:3
2Fa 17:35
Yer 25:6
f Kut 20:4
Law 26:1
Kum 4:16
Kum 4:23
Kum 27:15
g Mdo 17:29
h Kut 23:24
Da 3:18
1Ko 10:14
i Kut 34:14
Kum 4:24
Yos 24:19
Isa 42:8
Nah 1:2
Mt 4:10
j Kut 20:5
Kut 34:7
1Fa 21:29
Mt 23:35
k Kut 20:6
Yer 32:18
Da 9:4
Ro 11:28

Yehova na ninyi wakati huo[a]
ili kuwaambia neno la Yehova,
(kwa maana mliogopa kwa sa-
babu ya moto nanyi hamkupa-
nda juu mlimani,)[b] na kusema,
6 "'Mimi ni Yehova Mungu
wako,[c] niliyekutoa katika nchi
ya Misri, kutoka katika nyu-
mba ya watumwa.[d] **7** Usiwe
kamwe na miungu mingine dhi-
di ya uso wangu.[e]
8 "'Usijifanyie sanamu ya
kuchongwa,[f] umbo[g] lolote lili-
lo kama kitu chochote kili-
cho mbinguni juu au kilicho
duniani chini au kilicho kati-
ka maji chini ya dunia. **9** Usi-
viinamie wala kufanywa uvitu-
mikie,[h] kwa sababu mimi Yeho-
va Mungu wako ni Mungu ana-
yetaka watu wajitoe kikamili,[i]
ninayeleta adhabu kwa ajili ya
kosa la akina baba juu ya wana
na juu ya kizazi cha tatu na
juu ya kizazi cha nne, kwa wale
wanaonichukia;[j] **10** lakini ni-
nayeonyesha fadhili zenye upe-
ndo kwa kizazi cha elfu kwa
wale wanaonipenda na wanao-
shika amri zangu.[k]
11 "'Usilitumie jina la Yeho-
va Mungu wako katika njia ya
ubatili,[l] kwa maana Yehova ha-
tamwacha bila kumwadhibu,
yeyote ambaye analitumia jina
lake kwa njia isiyofaa.[m]
12 "'Kwa kuishika siku ya sa-
bato ili kuiona kuwa takatifu,
kama vile Yehova Mungu wako
alivyokuamuru,[n] **13** utatoa
utumishi nawe utafanya kazi
yako yote kwa siku sita.[o]
14 Lakini siku ya saba ni sa-
bato kwa Yehova Mungu wako.[p]
Usifanye kazi yoyote,[q] wewe
wala mwana wako wala binti
yako wala mtumishi wako wala

l Kut 20:7; Kut 22:28; Law 19:12; m Law 24:16; n Kut 16:23; Kut 20:8; Kut 31:13; o Kut 20:9; Kut 23:12; Kut 34:21; p Kut 16:29; q Ne 13:15.

kijakazi wako wala ng'ombe
wako wala mkaaji mgeni wako
aliye ndani ya malango yako,[a]
ili mtumishi wako na kijakazi
wako wapate kupumzika kama
wewe.[b] **15** Nawe ukumbuke
kwamba ulikuwa mtumwa kati-
ka nchi ya Misri[c] na Yehova Mu-
ngu wako akakutoa huko kwa
mkono wenye nguvu na kwa
mkono ulionyooshwa.[d] Ndiyo sa-
babu Yehova Mungu wako aliku-
amuru uendelee kuishika siku
ya sabato.[e]

16 "'Mheshimu baba yako na
mama yako,[f] kama vile amba-
vyo Yehova Mungu wako ame-
kuamuru; ili siku zako zipate
kuwa ndefu na ili mambo yaku-
endee vema[g] katika nchi amba-
yo Yehova Mungu wako anaku-
pa wewe.

17 "'Usiue.[h]

18 "'Wala usifanye uzinzi.[i]

19 "'Wala usiibe.[j]

20 "'Wala usimshuhudie
mwenzako uwongo.[k]

21 "'Wala usimtamani mke
wa mwenzako.[l] Wala usitama-
ni kwa uchoyo nyumba ya mwe-
nzako, shamba lake au mtu-
mishi wake au kijakazi wake,
ng'ombe wake au punda wake
au kitu chochote cha mwenza-
ko.'[m]

22 "Yehova aliliambia kuta-
niko lenu lote Maneno hayo ka-
tika mlima kutoka katikati ya
ule moto,[n] lile wingu na ule we-
usi mzito, kwa sauti kubwa,
naye hakuongeza lolote; ki-
sha akayaandika juu ya maba-
mba mawili ya mawe na kunipa
mimi.[o]

23 "Na ikawa kwamba mara
tu mlipoisikia sauti kutoka ka-
tikati ya lile giza, mlima uli-
pokuwa ukiwaka moto,[p] ninyi
mlikuja karibu nami, vichwa

SURA 5

a Kut 20:10
Kut 23:12
Law 24:22
b Kum 10:17
Ro 2:11
Efe 6:9
c Kum 15:15
Kum 24:18
d Kut 6:6
Kum 4:34
Isa 63:12
e Kut 31:17
f Kut 21:15
Law 19:3
Kum 27:16
Met 1:8
Mk 7:10
g Kut 20:12
Efe 6:3
h Mwa 9:6
Kut 20:13
Hes 35:21
Mt 5:21
Ro 13:9
i Kut 20:14
Met 6:32
1Ko 6:18
Ebr 13:4
j Kut 20:15
Law 19:11
Met 30:9
1Ko 6:10
Efe 4:28
k Kut 20:16
Kut 23:1
Law 19:16
Kum 19:16
Met 6:19
Met 19:5
l 2Sa 11:3
Mt 5:28
m Kut 20:17
1Fa 21:4
Lu 12:15
Ro 7:7
n Kut 19:9
Kut 19:18
Kum 4:12
o Kut 24:12
Kut 31:18
Kum 4:13
p Kut 20:18
Ebr 12:18

Safu ya 2

a Kut 19:18
Kut 24:17
Kum 4:36
b Kum 4:33
c Ebr 12:29
d Kut 20:19
Kum 18:16
Mdo 7:38
Ga 3:19
e Kum 4:33
Kum 5:5
Zb 29:4
1Th 1:9
f Kut 20:19
Ebr 12:19
g Kum 18:17
h Kum 10:12
Ayu 28:28
Met 1:7
Mt 10:28
1Pe 2:17
i Met 4:4
Met 7:2
Mhu 12:13
Isa 48:18
1Yo 5:3
j Zb 19:11
Yak 1:25

vyote vya makabila yenu na wa-
naume wenu wazee. **24** Ndi-
po mkasema, 'Tazama, Yeho-
va Mungu wetu ametuonyesha
utukufu wake na ukuu wake,
nasi tumeisikia sauti yake ku-
toka katikati ya moto.[a] Leo
tumeona kwamba Mungu ana-
weza kusema na mwanadamu
naye aendelee kuishi.[b] **25** Na
sasa kwa nini tufe, kwa maana
moto huu mkubwa unaweza ku-
tuteketeza?[c] Tukiisikia tena sa-
uti ya Yehova Mungu wetu, ha-
kika sisi tutakufa.[d] **26** Kwa
maana ni nani mwenye mwi-
li wa nyama ambaye ameisikia
sauti ya Mungu aliye hai[e] iki-
sema kutoka katikati ya moto
kama tulivyofanya sisi, naye
akaendelea kuishi? **27** Wewe
mwenyewe nenda karibu, usi-
kie yote ambayo Yehova Mu-
ngu wetu atasema; nawe ndiye
utakayesema nasi yote ambayo
Yehova Mungu wetu atasema
nawe,[f] nasi hakika tutasikiliza
na kuyatenda.'

28 "Kwa hiyo Yehova akaisi-
kia sauti ya maneno yenu mli-
posema nami, naye Yehova aka-
niambia, 'Nimeisikia sauti ya
maneno ya watu hawa, yale
ambayo wamekuambia. Wame-
fanya vema katika yote wa-
liyosema.[g] **29** Laiti wangaliu-
sitawisha moyo wao huu unio-
gope[h] na kushika amri zangu
zote sikuzote,[i] ili mambo yawa-
endee vema, wao na wana wao
mpaka wakati usio na kipi-
mo![j] **30** Nenda ukawaambie:
"Rudini nyumbani kwenye ma-
hema yenu." **31** Nawe usima-
me hapa pamoja nami, nami
nitasema nawe amri zote na
masharti na maamuzi ya hu-
kumu ambayo utawafundisha[k]

k Kum 4:45; Kum 6:1; Eze 20:11; Mal 4:4; Ga 3:19.

na ambayo watafanya katika
nchi nitakayowapa waimiliki.'
32 Nanyi mtakuwa waangalifu kufanya kama vile ambavyo
Yehova Mungu wenu amewaamuru ninyi.[a] Msigeuke kuume wala kushoto.[b] **33** Katika
njia yote ambayo Yehova Mungu wenu amewaamuru ninyi,
mnapaswa kutembea,[c] ili mpate kuishi na ili mambo yawaendee ninyi vema[d] nanyi mpate kurefusha siku zenu katika nchi mtakayoimiliki.

6 "Sasa hizi ndizo amri, masharti na maamuzi ya hukumu ambayo Yehova Mungu
wenu ameamuru mfundishwe,[e] ili myatende katika nchi mnayovuka ili kuimiliki; **2** upate kumwogopa[f] Yehova Mungu
wako ili kushika sheria zake zote na amri zake ambazo ninakuamuru wewe, wewe na mwana wako na mjukuu wako,[g] siku
zote za maisha yako, na ili siku zako ziwe ndefu.[h] **3** Nawe usikilize, Ee Israeli, nawe uwe
mwangalifu kuzitenda,[i] ili mambo yakuendee vema[j] nanyi mpate kuwa wengi sana, kama vile ambavyo Yehova Mungu
wa mababu zako amekuahidi wewe,[k] kuhusu nchi inayotiririka maziwa na asali.

4 "Sikiliza, Ee Israeli: Yehova Mungu wetu ni Yehova mmoja.[l] **5** Nawe lazima umpende Yehova Mungu wako
kwa moyo[m] wako wote na kwa nafsi[n] yako yote na kwa nguvu[o] zako zote. **6** Na maneno haya ninayokuamuru leo
lazima yawe moyoni mwako;[p] **7** nawe uyakazie kwa mwana wako[q] na kuyasema unapoketi katika nyumba yako na unapotembea barabarani na unapolala[r] na unapoamka. **8** Nawe
uyafunge kama ishara kwenye mkono wako,[a] na yawe kama utepe wa kipaji katikati ya macho yako;[b] **9** nawe uyaandike juu ya miimo ya mlango wa nyumba yako na juu ya malango yako.[c]

10 "Na itatukia kwamba Yehova Mungu wako atakapokuleta katika nchi ambayo aliwaapia mababu zako Abrahamu, Isaka na Yakobo, kwamba atakupa,[d] majiji makubwa na yenye kupendeza ambayo wewe
hukuyajenga,[e] **11** na nyumba zilizojaa vitu vyote vizuri na ambazo hukuzijaza, na mashimo ya maji yaliyochimbwa ambayo hukuyachimba, mashamba ya mizabibu
na mizeituni ambayo hukuipanda, nawe utakapokuwa umekula na kushiba,[f] **12** jiangalie usije ukamsahau[g] Yehova, aliyekutoa katika nchi ya
Misri, kutoka katika nyumba ya watumwa. **13** Unapaswa kumwogopa Yehova Mungu wako,[h] nawe unapaswa
kumtumikia yeye,[i] nawe unapaswa kuapa kwa jina lake.[j]
14 Usiifuate miungu mingine, miungu yoyote ya vikundi vya watu wanaowazunguka pande
zote,[k] **15** (kwa maana Yehova Mungu wako aliye katikati yako ni Mungu anayetaka watu wajitoe kikamili,)[l] hasira ya Yehova isije ikawaka juu yako,[m]
naye akuangamize kutoka katika uso wa nchi.[n]

16 "Msimjaribu Yehova Mungu wenu,[o] vile mlivyomjaribu huko Masa.[p] **17** Mnapaswa kuzishika kwa vyovyote
amri za Yehova Mungu[q] wenu

SURA 5
a Kum 6:3
Kum 6:25
Kum 8:1
b Kum 12:32
Yos 1:7
Met 4:27
c Kum 10:12
Yer 7:23
d Kum 4:40
Kum 12:28
Met 19:16
Ro 10:5

SURA 6
e Kum 4:1
Kum 4:10
f Kut 20:20
Yos 24:14
Ayu 28:28
Zb 111:10
Zb 128:1
g Mwa 18:19
Kum 4:9
h Kum 5:16
Met 3:2
i Kum 5:32
2Fa 21:8
j Mhu 8:12
Isa 3:10
k Mwa 13:16
l Kum 5:7
Isa 42:8
Zek 14:9
Mk 12:29
1Ko 8:6
m Kum 10:12
Mt 22:37
n Kum 11:13
Kum 30:6
o Mk 12:30
Lu 10:27
p Kum 11:18
Met 7:3
q Mwa 18:19
Kum 4:9
Kum 11:19
Met 22:6
Efe 6:4
r Met 6:22

Safu ya 2
a Met 3:3
Met 7:3
b Kut 13:9
Kut 13:16
Kum 11:18
c Kum 11:20
d Mwa 15:18
e Yos 24:13
Zb 105:44
f Kum 8:10
g Amu 3:7
Yer 2:32
h Kum 10:12
Kum 13:4
Zb 34:9
Zb 128:1
i Lu 4:8
j Kum 10:20
Amu 21:7
Yer 12:16
k Kut 34:14
Kum 8:19
Yer 25:6
l Kut 20:5
Kum 4:24
Yos 24:19
Nah 1:2
m Kut 32:10
Hes 25:3
Kum 11:17
Amu 2:14
n 1Fa 13:34
2Fa 17:18

o Mt 4:7; Lu 4:12; 1Ko 10:9; p Kut 17:2; Kum 33:8; Zb 95:8; Ebr 3:8; q Kum 11:13; Eze 20:11.

na ushuhuda[a] wake na masharti[b] yake ambayo amekuamuru.[c] **18** Nawe ufanye yaliyo sawa na yaliyo mema machoni pa Yehova, ili mambo yakuendee vema[d] wewe, nawe kwa kweli upate kuingia na kumiliki ile nchi nzuri ambayo Yehova amewaapia mababu zako,[e] **19** kwa kuwasukumia mbali adui zako wote toka mbele yako, kama vile ambavyo Yehova ameahidi.[f]

20 "Ikiwa mwana wako atakuuliza katika siku fulani wakati ujao,[g] akisema, 'Ushuhuda na masharti na maamuzi ya hukumu ambayo Yehova Mungu wetu amewaamuru ninyi yanamaanisha nini?' **21** ndipo utakapomwambia mwana wako, 'Tulikuwa watumwa kwa Farao katika Misri, lakini Yehova alitutoa Misri kwa mkono wenye nguvu.[h] **22** Basi Yehova akaendelea kuweka ishara na miujiza,[i] kubwa na zenye kuleta msiba, juu ya Misri, juu ya Farao na juu ya nyumba yake yote mbele ya macho yetu.[j] **23** Naye akatutoa huko ili atulete hapa, atupe nchi ambayo alikuwa amewaapia mababu zetu.[k] **24** Basi Yehova akatuamuru tushike masharti yote haya,[l] tumwogope Yehova Mungu wetu kwa ajili ya hali njema yetu sikuzote,[m] ili tupate kuendelea kuwa hai kama ilivyo leo hii.[n] **25** Nayo itamanisha uadilifu kwetu,[o] kwamba tuwe waangalifu kutenda amri yote hii mbele za Yehova Mungu wetu, kama vile ambavyo ametuamuru.'[p]

7 "Wakati ambapo Yehova Mungu wako mwishowe atakuingiza katika nchi ambayo unaenda kuimiliki,[q] pia atao-

SURA 6

a 1Fa 2:3
b Kum 4:1
Ne 9:13
c Kum 11:22
Zb 119:4
d Kum 5:33
e Mwa 15:18
f Kut 23:30
Hes 33:52
g Kut 13:14
h Kut 15:6
i Kut 7:3
Kum 7:19
j Kum 4:34
k Kut 13:5
Kum 1:8
l Kum 5:1
1Fa 2:3
m Kum 10:12
Zb 111:10
Met 14:27
Mhu 8:12
n Kum 4:1
Lu 10:28
Ga 3:12
o Ro 10:5
p Law 18:5
Mhu 12:13

SURA 7

q Kum 31:3
Zb 44:2

Safu ya 2

a Kut 33:2
Yos 3:10
b Mwa 10:15
c Mwa 10:16
d Mwa 15:16
e Mwa 10:19
f Yos 11:3
g Mwa 10:17
h 1Nya 1:14
i Kum 20:1
j Hes 33:52
Mdo 13:19
k Law 27:29
Kum 20:17
Yos 6:17
Yos 10:28
l Kut 23:32
Kut 34:15
Kum 20:16
Amu 2:2
m Yos 23:12
1Fa 11:2
Ezr 9:2
Ne 10:30
n Kut 34:16
1Fa 11:4
o Kum 6:15
p Kut 34:13
Kum 12:2
q Kut 23:24
Kum 12:3
Kum 16:22
r Kum 16:21
s Amu 6:25
t Kum 7:25
Kum 12:3
u Kut 19:6
Kum 14:2
Yer 2:3
v Kut 19:5
Zb 135:4
Amo 3:2
Mal 3:17
w Kum 4:37
Kum 10:15
Zb 105:6
Ro 9:11
x Kum 10:22
Zb 105:12
Isa 51:2

ndolea mbali mataifa yenye hesabu kubwa ya watu toka mbele yako,[a] Wahiti[b] na Wagirgashi[c] na Waamori[d] na Wakanaani[e] na Waperizi[f] na Wahivi[g] na Wayebusi,[h] mataifa saba yenye hesabu kubwa ya watu na yenye nguvu kuliko wewe.[i] **2** Na Yehova Mungu wako hakika atawatia hao mkononi mwako, nawe utawashinda.[j] Unapaswa kuwaangamiza.[k] Usifanye agano lolote pamoja nao wala kuwaonyesha kibali chochote.[l] **3** Nawe usifanye mapatano yoyote ya ndoa pamoja nao. Binti yako usimpe mwana wake, wala binti yake usimchukue kwa ajili ya mwana wako.[m] **4** Kwa maana atamgeuza mwana wako aache kunifuata, nao watatumikia miungu mingine;[n] na hasira ya Yehova itawaka kwelikweli juu yenu, naye hakika atakuangamiza haraka.[o]

5 "Kwa upande mwingine, hivi ndivyo mtakavyowafanyia: Madhabahu zao mtazibomoa,[p] nazo nguzo zao takatifu mtazivunja,[q] nayo miti yao mitakatifu[r] mtaikata,[s] na sanamu zao za kuchongwa mtaziteketeza kwa moto.[t] **6** Kwa maana ninyi ni watu watakatifu kwa Yehova Mungu wenu.[u] Ni ninyi ambao Yehova Mungu amewachagua ninyi muwe watu wake, mali ya pekee, kutoka kati ya vikundi vyote vya watu vilivyo kwenye uso wa nchi.[v]

7 "Yehova hakuwaonyesha upendo hivi kwamba akawachagua kwa sababu mlikuwa kikundi chenye hesabu kubwa zaidi ya watu kuliko vikundi vyote,[w] kwa maana ninyi ndio mliokuwa kikundi chenye watu wachache zaidi.[x]

8 Lakini ilikuwa kwa sababu
Yehova aliwapenda ninyi,[a] na
kwa sababu ya kushika ile aha-
di yenye kiapo aliyowaapia ma-
babu zenu,[b] ndiyo sababu Ye-
hova aliwatoa nje kwa mkono
wenye nguvu,[c] apate kuwako-
moboa ninyi kutoka katika nyu-
mba ya watumwa,[d] kutoka kati-
ka mkono wa Farao mfalme wa
Misri. **9** Nawe unajua vema
kwamba Yehova Mungu wako
ndiye Mungu wa kweli,[e] yule
Mungu mwaminifu,[f] anayeshi-
ka agano[g] na fadhili zenye upe-
ndo kwa wale wanaompenda
na wale wanaoshika amri zake
mpaka vizazi elfu,[h] **10** laki-
ni anayemlipa usoni pake yule
anayemchukia kwa kumwa-
ngamiza.[i] Hatasitasita kuele-
kea yule anayemchukia; ata-
mlipa usoni pake. **11** Nawe
utashika amri na masharti na
maamuzi ya hukumu ninayoku-
amuru leo kwa kuyatenda.[j]

12 "Na itatukia kwamba,
kwa sababu mnaendelea kusi-
kiliza maamuzi haya ya huku-
mu na kuyashika na kuyateke-
leza,[k] Yehova Mungu wako ata-
kutimizia lile agano[l] na fadhili
zenye upendo ambazo aliwaa-
pia mababu zako.[m] **13** Naye
hakika atakupenda na kuku-
bariki[n] na kukuzidisha[o] na ku-
bariki uzao wa tumbo lako[p]
na mazao ya udongo wako,[q] na-
faka yako na divai yako mpya
na mafuta yako, watoto wa
ng'ombe wako na uzao wa ku-
ndi lako,[r] kwenye nchi aliyowa-
apia mababu zako ya kwamba
atakupa wewe.[s] **14** Utakuwa
kikundi cha watu kilichobari-
kiwa zaidi kuliko vikundi vi-
ngine vyote.[t] Katikati yako
hapatakuwa na mwanamume
au mwanamke asiye na uzao,

SURA 7

a Kum 23:5
b Mwa 22:16
Kut 32:13
Kum 10:15
Zb 105:9
Lu 1:73
c Kut 13:14
d Kut 6:6
Kut 13:3
Isa 51:10
e Law 26:45
Kum 4:35
Zb 68:20
f Isa 49:7
1Ko 10:13
2Ko 1:18
Ebr 11:11
g Ne 1:5
Da 9:4
h Kut 34:7
Kum 5:10
i Zb 21:9
Zb 68:2
Met 2:22
Isa 59:18
Nah 1:2
2Pe 3:7
j Kum 5:32
Yoh 13:17
Yak 1:22
k Kut 15:26
Kum 28:1
l Zb 105:8
m Mik 7:20
Lu 1:55
Lu 1:72
n Kut 23:25
Met 10:22
o Law 26:9
p Kum 28:4
q Law 26:4
r Zb 107:38
s Mwa 13:15
t Kum 33:29
Zb 115:15
Zb 147:20

Safu ya 2

a Kut 23:26
Kum 28:11
Zb 127:3
b Kum 28:27
Kum 28:60
Amo 4:10
c Kum 7:2
Kum 20:16
Yos 10:28
d Mwa 15:16
Law 18:25
Kum 9:5
e Kut 20:3
f Kut 23:33
Kum 12:30
Amo 2:3
Zb 106:36
g Hes 13:31
h Kum 1:29
Kum 31:6
Zb 27:1
Isa 41:10
i Kut 14:13
Zb 105:27
Zb 135:8
Mdo 13:17
j Kum 29:3
Ne 9:11
k Ne 9:10
Yer 32:20
l Kut 13:3
m Kum 11:2
n Kum 4:34
o Kut 23:28
Yos 3:10
p Kum 2:25
Yos 2:9
Yos 24:12

wala katikati ya wanyama wako
wa kufugwa.[a] **15** Na Yehova
atakuondolea kila ugonjwa;
na yale magonjwa mabaya ya
Misri unayoyajua,[b] hatayawe-
ka juu yako, naye atayawe-
ka juu ya wote wanaokuchu-
kia. **16** Nawe utawaangamiza
watu wote ambao Yehova Mu-
ngu wako anawatia mkononi
mwako.[c] Jicho lako lisiwasikiti-
kie;[d] wala usiitumikie miungu
yao,[e] kwa sababu jambo hilo li-
takuwa mtego kwako.[f]

17 "Ikiwa utasema moyoni
mwako, 'Mataifa haya yana
watu wengi mno kwangu. Ni-
tawezaje kuyafukuzia mbali?'[g]
18 usiwaogope.[h] Kumbuka ka-
bisa yale ambayo Yehova Mu-
ngu wako alimtendea Farao na
Misri yote,[i] **19** ule uthibitisho
mkubwa ambao macho yako ya-
liona,[j] na zile ishara na miuji-
za[k] na ule mkono wenye nguvu[l]
na ule mkono ulionyooshwa[m]
ambao Yehova Mungu wako
aliutumia kukutoa huko.[n] Hi-
vyo ndivyo Yehova Mungu
wako atakavyowatendea watu
wote unaoogopa mbele yao.[o]
20 Na Yehova Mungu wako pia
atapeleka juu yao hisia ya ku-
vunjika moyo,[p] mpaka wale wa-
liobaki[q] na waliojificha mbele
yako waangamie. **21** Usishtu-
ke kwa sababu yao, kwa maana
Yehova Mungu wako yuko ka-
tikati yako,[r] Mungu mkuu na
mwenye kuogopesha.[s]

22 "Na Yehova Mungu wako
atayasukumia mbali mataifa
haya toka mbele yako kido-
go kidogo.[t] Hutaruhusiwa ku-
wamaliza kabisa upesi, wanya-
ma wa mwituni wasije wakao-

q Kut 23:29; r Hes 14:9; Zb 46:5; s Kum 10:17; 1Sa 4:8; Ne 1:5; Ne 9:32; t Kut 23:30.

ngezeka dhidi yako. **23** Na Yehova Mungu wako atawatia mkononi mwako na kuwashinda kabisa kwa ushindi mkubwa, mpaka wawe wameangamizwa.[a] **24** Naye atawatia wafalme wao mkononi mwako,[b] nawe lazima uyaharibu majina yao toka chini ya mbingu.[c] Hakuna mtu atakayesimama imara dhidi yako,[d] mpaka utakapokuwa umewaangamiza.[e] **25** Sanamu za kuchongwa za miungu yao mtaziteketeza kwa moto.[f] Usitamani fedha na dhahabu iliyo juu yake,[g] wala usiichukue kwa ajili yako,[h] usije ukanaswa nayo;[i] kwa maana hizo ni chukizo[j] kwa Yehova Mungu wako. **26** Nawe usilete chukizo katika nyumba yako nawe uwe kitu kilichotengwa kwa ajili ya kuangamizwa kama kitu hicho. Kinai kitu hicho na kukichukia kabisa,[k] kwa sababu ni kitu kilichotengwa kwa ajili ya kuangamizwa.[l]

8 "Kila amri ninayokuamuru leo muwe waangalifu kuishika,[m] ili mpate kuendelea kuishi[n] na kuongezeka, mwingie na kuimiliki nchi ambayo Yehova aliwaapia mababu zenu.[o] **2** Nawe uikumbuke njia yote ambayo Yehova Mungu wako alikutembeza miaka hii 40 nyikani,[p] ili kukunyenyekeza,[q] kukujaribu[r] apate kujua yaliyokuwa moyoni mwako,[s] iwapo utashika amri zake au hapana. **3** Kwa hiyo alikunyenyekeza, akakuacha ukae na njaa,[t] akakulisha mana,[u] ambayo hukuwa umeijua wala baba zako hawakuwa wameijua; ili kukufanya ujue kwamba mwanadamu haishi kwa mkate tu bali mwanadamu huishi kwa kila neno la kinywa cha Yehova.[a] **4** Nguo yako ya kujitanda haikuchakaa, wala mguu wako haukuvimba miaka hii 40.[b] **5** Nawe unajua vema kwa moyo wako mwenyewe kwamba kama vile mtu anavyomrekebisha mwana wake, ndivyo Yehova Mungu wako alikuwa akikurekebisha.[c]

6 "Nawe ushike amri za Yehova Mungu wako kwa kutembea katika njia zake[d] na kwa kumwogopa.[e] **7** Kwa maana Yehova Mungu wako anakuleta katika nchi nzuri,[f] nchi yenye mabonde ya mito yenye maji, mabubujiko na vilindi vya maji kutoka katika nchi tambarare ya bonde[g] na katika eneo lenye milima, **8** nchi ya ngano na shayiri na mizabibu na tini na makomamanga,[h] nchi ya mizeituni ya mafuta na asali,[i] **9** nchi ambamo hutakula mkate kwa uhaba, ambamo hutakosa chochote, nchi ambayo mawe yake ni chuma na ambayo kutoka katika milima yake utachimba shaba.

10 "Utakapokuwa umekula na kushiba,[j] wewe pia unapaswa kumbariki[k] Yehova Mungu wako kwa ajili ya mema ya nchi ambayo amekupa.[l] **11** Jiangalie usije ukamsahau[m] Yehova Mungu wako kwa kutozishika amri zake na maamuzi yake ya hukumu na sheria zake ambazo ninakuamuru leo;[n] **12** usije ukala na kushiba kwelikweli, ukajenga nyumba nzuri na kukaa ndani yake,[o] **13** na mifugo yako na kundi lako likaongezeka, na fedha na dhahabu zikakuongezekea, na vyote vilivyo vyako vikaongezeka; **14** nao moyo wako uinuke juu,[p] na umsahau Yehova Mungu wako,

SURA 7

a Kum 9:3
b Yos 10:24
Yos 12:1
c Kut 17:14
Zb 9:5
d Kum 11:25
Yos 1:5
Yos 23:9
Ro 8:31
e Yos 11:14
f Kut 32:20
Kum 12:3
1Nya 14:12
g Isa 30:22
h Yos 7:21
i Kum 7:16
Amu 8:27
j Kum 27:15
Kum 29:17
k Ro 2:22
l Law 27:28
Kum 13:17

SURA 8

m Kum 5:32
Zb 119:4
1Th 4:1
n Met 3:2
o Mwa 15:18
p Kum 2:7
Kum 29:5
Amo 2:10
q Zb 101:5
Lu 18:14
1Pe 5:6
r Kut 16:4
Kut 20:20
s Kum 13:3
Zb 139:23
Met 17:3
t Kut 16:3
u Kut 16:31
Zb 78:24

Safu ya 2

a Mt 4:4
b Kum 29:5
Ne 9:21
c 2Sa 7:14
Met 3:12
1Ko 11:32
Ebr 12:6
Ufu 3:19
d Kum 5:33
2Nya 6:31
Zb 128:1
Lu 1:6
e 1Sa 12:24
f Kut 3:8
Law 26:4
Kum 11:12
Ne 9:25
g Kum 11:11
h Hes 13:23
i Eze 20:6
j Kum 6:11
k Zb 103:2
Zb 134:1
l 1Nya 29:14
m Zb 106:21
n Kum 6:12
o Kum 32:15
Yer 22:14
Ho 13:6
p Kum 9:4
1Ko 4:7

aliyekutoa katika nchi ya Misri, kutoka katika nyumba ya watumwa;[a] **15** aliyekutembeza katika ile nyika kubwa na yenye kuogopesha,[b] iliyo na nyoka wenye sumu[c] na nge na nchi kame ambayo haina maji; ambaye alikutolea maji katika jiwe gumu;[d] **16** aliyekulisha mana[e] nyikani, ambayo baba zako hawakuwa wameijua, apate kukunyenyekeza[f] na kukujaribu ili akutendee mema siku zako za baadaye;[g] **17** nawe useme moyoni mwako, 'Nguvu zangu mwenyewe na uwezo kamili wa mkono wangu mwenyewe zimenifanyizia mali hii.'[h] **18** Nawe umkumbuke Yehova Mungu wako, kwa sababu yeye ndiye anayekupa nguvu za kufanyiza mali;[i] ili kutimiza agano lake ambalo aliwaapia mababu zako, kama ilivyo leo hii.[j]

19 "Na itatukia kwamba ikiwa utamsahau Yehova Mungu wako hata kidogo nawe ufuate miungu mingine na kuitumikia na kuiinamia, nashuhudia juu yenu leo kwamba ninyi mtaangamia kabisa.[k] **20** Kama yale mataifa ambayo Yehova anaangamiza kutoka mbele yenu, hivyo ndivyo mtakavyoangamia, kwa sababu ninyi hamtaisikiliza sauti ya Yehova Mungu wenu.[l]

9 "Sikia, Ee Israeli, leo unavuka Yordani[m] uingie ndani na kuyafukuza mataifa makubwa zaidi na yenye nguvu zaidi kuliko wewe,[n] majiji makubwa na yenye ngome zinazofika mbinguni,[o] **2** watu wakubwa na warefu, wana wa Waanaki,[p] ambao umejua na kusikia ikisemwa juu yao, 'Ni nani anayeweza kusimama imara mbele ya wana wa Anaki?' **3** Nawe unajua vema leo kwamba Yehova Mungu wako anavuka mbele yako.[a] Yeye ni moto unaoteketeza.[b] Atawaangamiza hao,[c] na yeye mwenyewe atawatiisha mbele yenu; nanyi mtawafukuza na kuwaharibu haraka, kama vile ambavyo Yehova amesema nanyi.[d]

4 "Usiseme hivi moyoni mwako wakati ambapo Yehova Mungu wako atawasukumia mbali kutoka mbele yako, 'Kwa sababu ya uadilifu wangu mwenyewe Yehova amenileta ndani niimiliki nchi hii,'[e] ingawa ni kwa sababu ya uovu wa mataifa haya kwamba Yehova anawafukuzia mbali kutoka mbele yako.[f] **5** Hutaimiliki nchi yao kwa sababu ya uadilifu[g] wako wala kwa sababu ya unyoofu wa moyo wako;[h] kwa kweli, Yehova anayafukuzia mbali mataifa haya kutoka mbele yako[i] kwa sababu ya uovu wao, na ili kulitimiza neno ambalo Yehova aliwaapia mababu zako, Abrahamu,[j] Isaka[k] na Yakobo.[l] **6** Nawe ni lazima ujue kwamba Yehova Mungu wako hakupi wewe nchi hii nzuri uimiliki kwa sababu ya uadilifu wako; kwa maana ninyi ni watu wenye shingo ngumu.[m]

7 "Kumbuka: Usisahau jinsi ambavyo umemchokoza Yehova Mungu wako nyikani.[n] Tangu siku uliyotoka katika nchi ya Misri mpaka mlipofika mahali hapa ninyi mmekuwa wenye tabia ya kumwasi Yehova.[o] **8** Hata katika Horebu mlimfanya Yehova akasirike hivi kwamba Yehova akapandwa na hasira kufikia hatua ya kuwaangamiza ninyi.[p] **9** Nilipoe-

SURA 8

a Zb 106:21
b Kum 1:19
Yer 2:6
c Hes 21:6
d Hes 20:11
Zb 78:15
Zb 105:41
Zb 114:8
1Ko 10:4
e Kut 16:35
Yoh 6:31
Yoh 6:49
f Kum 8:2
g 2Ko 4:17
Ebr 12:11
1Pe 1:7
h Ho 12:8
Hab 1:16
1Ko 4:7
i Zb 127:1
Met 10:22
Ho 2:8
j Kum 7:12
k Kum 4:26
Kum 30:18
Yos 23:13
1Sa 12:25
l Da 9:11
Da 9:12
Amo 3:2

SURA 9

m Kum 11:31
Yos 4:19
n Kum 4:38
Kum 7:1
Kum 11:23
o Hes 13:28
p Hes 13:33
Kum 1:28
Kum 2:21

Safu ya 2

a Kum 1:30
Kum 20:4
Kum 31:3
Yos 3:11
b Kum 4:24
Nah 1:6
Ebr 12:29
c Kum 7:23
Kum 20:16
d Kut 23:31
Kum 7:24
e Kum 7:8
Eze 36:22
f Mwa 15:16
Kum 12:31
Kum 18:12
g 1Fa 8:46
Zb 51:5
Ro 3:23
Ro 5:12
Tit 3:5
h Yer 17:9
i Law 18:25
j Mwa 13:15
Mwa 17:8
k Mwa 26:3
l Mwa 28:13
m Kut 34:9
Zb 78:8
Isa 48:4
Mdo 7:51
n Kum 9:22
Zb 78:40
Ebr 3:16

o Kut 17:2; Hes 11:4; Hes 16:2; Hes 25:2; Kum 31:27; Kum 32:5; Ne 9:16; p Kut 32:4; Kut 32:10; Zb 106:19.

nda juu mlimani nikapokee
yale mabamba ya mawe,[a] ma-
bamba ya agano ambalo Ye-
hova alikuwa amefanya pamo-
ja nanyi,[b] nami nikaendelea ku-
kaa mlimani siku 40, mchana
na usiku,[c] (sikula mkate wala
kunywa maji,) **10** kisha Yeho-
va akanipa yale mabamba ma-
wili ya mawe yaliyoandikwa
kwa kidole cha Mungu;[d] na ma-
neno yote ambayo Yehova ali-
kuwa amesema nanyi katika
mlima kutoka katikati ya moto
katika siku ya kutaniko, yali-
kuwa juu yake.[e] **11** Na ika-
wa kwamba mwishoni mwa zile
siku 40, mchana na usiku, Ye-
hova akanipa yale mabamba
mawili ya mawe, mabamba ya
agano;[f] **12** na Yehova akania-
mbia, 'Ondoka, shuka upesi
kutoka hapa, kwa sababu watu
wako uliowatoa Misri wamete-
nda kwa uharibifu.[g] Wamege-
uka kando upesi kutoka katika
njia ambayo niliwaamuru.
Wamejifanyia wenyewe sana-
mu ya kuyeyushwa.'[h] **13** Naye
Yehova akaniambia hivi, 'Ni-
mewaona watu hawa, na, taza-
ma! ni watu wenye shingo ngu-
mu.[i] **14** Niache nipate kuwaa-
ngamiza[j] na kufagilia mbali jina
lao kutoka chini ya mbingu,[k] na
acha nikufanye wewe kuwa tai-
fa lenye nguvu zaidi na lenye he-
sabu kubwa zaidi ya watu kuliko
walivyo.'[l]

15 "Kisha nikageuka na ku-
shuka kutoka mlimani, huku
mlima ukiwaka moto;[m] na yale
mabamba mawili ya agano yali-
kuwa katika mikono yangu mi-
wili.[n] **16** Halafu nikaangalia,
na tazama, ninyi mlikuwa
mmemtendea dhambi Yehova
Mungu wenu! Mlikuwa mmeji-
fanyia wenyewe ndama wa ku-
yeyushwa.[a] Mlikuwa mmegeu-
ka kando upesi kutoka katika
njia ambayo Yehova alikuwa
amewaamuru ninyi.[b] **17** Ndi-
po nikashika yale mabamba
mawili, nikayatupa chini kuto-
ka katika mikono yangu miwi-
li, nikayavunja mbele ya ma-
cho yenu.[c] **18** Nami nikajila-
za kifudifudi mbele za Yehova,
kama mara ya kwanza, siku 40,
mchana na usiku. Sikula mka-
te wala kunywa maji,[d] kwa sa-
babu ya dhambi zenu zote mli-
zokuwa mmetenda kwa kute-
nda uovu machoni pa Yehova
ili kumtia uchungu.[e] **19** Kwa
maana niliogopa kwa sababu ya
hasira kali ambayo Yehova ali-
kuwa ameghadhibika kuwaele-
kea ninyi kufikia hatua ya ku-
waangamiza ninyi.[f] Hata hivyo,
Yehova alinisikiliza pia wakati
huo.[g]

20 "Yehova pia akamkasiri-
kia sana Haruni kufikia ha-
tua ya kumwangamiza;[h] laki-
ni niliomba dua[i] pia kwa ajili
ya Haruni wakati huo.
21 Nayo dhambi yenu mliyoite-
nda, yule ndama,[j] nilimchukua,
nikamteketeza katika moto na
kumponda-ponda, nikamsaga
kabisa mpaka akawa mavumbi
laini; kisha nikayatupa mavu-
mbi yake katika mto unaotere-
mka kutoka mlimani.[k]

22 "Na zaidi ya hayo, huko
Tabera[l] na huko Masa[m] na huko
Kibroth-hataava[n] mlimkasiri-
sha Yehova.[o] **23** Na Yehova ali-
powatuma kutoka Kadesh-
barnea,[p] na kusema, 'Pande-
ni mwimiliki nchi ambayo nita-
wapa ninyi!' ndipo mkaasi agizo
la Yehova Mungu wenu,[q] nanyi
hamkumwamini[r] wala hamkui-
sikiliza sauti yake.[s] **24** Mmeji-
onyesha kuwa wenye tabia ya

SURA 9

a Kut 24:12
Kut 31:18
Kut 32:16
b Kut 24:7
Ga 4:24
c Kut 24:18
d Kut 31:18
Zb 8:3
Mt 12:28
Lu 11:20
e Kut 19:19
Kum 4:10
Kum 4:12
f Kut 31:18
Kum 4:13
g Kut 32:7
Kum 4:16
h Kut 32:4
i Kut 32:9
j Kut 32:10
k Kum 7:24
Zb 9:5
l Hes 14:12
m Kut 19:18
Kum 4:11
n Kut 32:15

Safu ya 2

a Mdo 7:40
b Kut 20:3
Kut 20:4
Kum 5:8
Mdo 7:41
c Kut 32:19
d Kut 34:28
e Ne 9:18
f Kut 32:10
g Kut 32:11
Kut 32:14
Kum 10:10
Zb 106:23
h Kut 32:2
Kut 32:21
Kut 32:35
i Met 15:29
Yak 5:16
j Kut 32:4
k Kut 32:20
Isa 30:22
l Hes 11:3
m Kut 17:7
Kum 6:16
n Hes 11:4
Hes 11:34
o Kum 9:7
p Hes 13:26
Kum 1:19
q Hes 14:3
Hes 14:4
Isa 63:10
r Kum 1:32
Zb 106:24
Ebr 3:19
s Zb 106:25

kumwasi Yehova[a] tangu siku niliyowajua ninyi.

25 "Kwa hiyo nikaendelea kujilaza kifudifudi mbele za Yehova siku 40, mchana na usiku,[b] kwa maana nilijilaza kifudifudi hivyo kwa sababu Yehova alizungumza juu ya kuwaangamiza ninyi.[c] **26** Nami nikaanza kuomba dua[d] kwa Yehova na kusema, 'Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, usiwaharibu watu wako, mali yako binafsi,[e] uliowakomboa kwa ukuu wako, ambao uliwatoa Misri[f] kwa mkono wenye nguvu.[g] **27** Uwakumbuke watumishi wako Abrahamu, Isaka na Yakobo.[h] Usiugeuze uso wako kuelekea ugumu wa watu hawa na uovu wao na dhambi yao,[i] **28** ili nchi[j] uliyotutoa ndani yake isije ikasema: "Kwa sababu Yehova hakuweza kuwaingiza katika nchi aliyokuwa amewaapia, na kwa sababu aliwachukia, ndiyo maana aliwatoa ili apate kuwaua nyikani."[k] **29** Wao pia ni watu wako na mali yako[l] binafsi ambayo ulitoa kwa nguvu zako kuu na kwa mkono wako ulionyooshwa.'[m]

10 "Wakati huo Yehova aliniambia, 'Jichongee mabamba mawili ya mawe kama yale ya kwanza,[n] nawe uje kwangu juu mlimani, nawe utajitengenezea sanduku la mbao.[o] **2** Nami nitaandika juu ya mabamba hayo yale maneno yaliyokuwa kwenye yale mabamba ya kwanza, ambayo uliyavunja, nawe utayaweka ndani ya sanduku hilo.' **3** Kwa hiyo nikatengeneza sanduku la mbao za mshita, nikachonga mabamba mawili ya mawe kama yale ya kwanza[p] na kupanda juu mlimani, nayo yale mabamba mawili yalikuwa mkononi mwangu. **4** Kisha akaandika juu ya yale mabamba maandishi yaleyale kama ya kwanza,[a] yale Maneno Kumi,[b] ambayo Yehova alisema nanyi mlimani toka katikati ya moto[c] katika siku ya kutaniko;[d] kisha Yehova akanipa hayo. **5** Ndipo nikageuka, nikashuka kutoka mlimani[e] na kuweka yale mabamba katika sanduku nililokuwa nimetengeneza, ili yapate kukaa humo, kama vile ambavyo Yehova alikuwa ameniamuru.[f]

6 "Nao wana wa Israeli wakaondoka Beerothi Bene-yaakani[g] wakielekea Mosera. Huko Haruni akafa, naye akazikwa huko;[h] na Eleazari mwana wake akawa kuhani badala yake.[i] **7** Kutoka huko wakaondoka kuelekea Gudgoda, na kutoka Gudgoda kuelekea Yotbata,[j] nchi yenye mabonde ya mito yenye maji yanayotiririka.

8 "Wakati huo Yehova alitenga kabila la Lawi[k] ili lichukue sanduku la agano la Yehova,[l] lisimame mbele za Yehova ili kumhudumia[m] na kubariki katika jina lake mpaka leo hii.[n] **9** Ndiyo sababu Lawi hana fungu na urithi pamoja na ndugu zake.[o] Yehova ndiye urithi wake, kama vile Yehova Mungu wako alivyokuwa amemwambia.[p] **10** Na mimi—mimi nilikaa mlimani kama siku za kwanza, siku 40, mchana na usiku,[q] naye Yehova akanisikiliza pia katika pindi hiyo.[r] Yehova hakutaka kukuharibu wewe.[s] **11** Ndipo Yehova akaniambia, 'Ondoka, nenda mbele ya watu ili watoke, wapate kuingia na kuimiliki nchi ambayo nimewa-

SURA 9

a Kum 31:27; Mdo 7:51
b Kut 34:28; Kum 9:18; Mt 4:2
c Kum 9:19
d Zb 99:6; Met 15:29; Yak 5:16
e Kut 19:5; Kum 32:9; Zb 135:4; Amo 3:2
f 1Fa 8:51
g Kut 32:11; Zb 99:6
h Kut 3:6; Kut 6:8; Kum 9:5
i Kut 32:31; Zb 78:8; Mik 7:18
j Kum 5:6
k Kut 32:12; Hes 14:16; Zb 115:2
l Kum 4:20; 1Fa 8:51; Ne 1:10; Zb 74:2; Zb 95:7; Zb 100:3
m Kut 6:6; Kum 4:34; Isa 63:12

SURA 10

n Kut 34:1
o Kum 10:3
p Kut 34:4

Safu ya 2

a Kut 32:15; Kut 34:28
b Kut 20:1; Kum 4:13
c Kum 4:36; Kum 5:4
d Kut 19:17; Kum 5:22
e Kut 34:29
f Kum 10:2
g Hes 33:31
h Hes 20:23; Hes 20:24; Hes 33:38
i Hes 20:28
j Hes 33:33
k Hes 1:50; Hes 3:6; Hes 8:14; Hes 16:9
l Hes 3:31; Hes 4:15; 1Nya 15:15
m Kum 18:5; 2Nya 29:11
n Hes 6:23; Kum 21:5; 2Nya 30:27
o Hes 18:24; Hes 26:62; Kum 18:1
p Hes 18:20
q Kut 24:18; Kut 34:28
r Kut 32:14
s Eze 33:11

apia mababu zao kwamba nitawapa wao.'[a]

12 "Na sasa, Ee Israeli, Yehova Mungu wako anataka nini kutoka kwako[b] ila kumwogopa[c] Yehova Mungu wako, ili kutembea katika njia zake zote[d] na kumpenda[e] yeye na kumtumikia Yehova Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa nafsi yako yote;[f] **13** kuzishika amri za Yehova na sheria[g] zake ninazokuamuru wewe leo, kwa faida yako?[h] **14** Tazama, mbingu, naam, mbingu za mbingu,[i] dunia[j] na vyote vilivyomo, ni mali ya Yehova. **15** Ila Yehova alishikamana na mababu zako na kuwapenda, hivi kwamba akachagua uzao wao baada yao,[k] naam, ninyi, kutoka kati ya vikundi vyote vya watu, kama ilivyo leo hii. **16** Nanyi mtatahiri govi la mioyo[l] yenu wala msifanye shingo zenu kuwa ngumu tena.[m] **17** Kwa maana Yehova Mungu wenu ni Mungu wa miungu[n] na Bwana wa mabwana,[o] Mungu mkuu, mwenye nguvu na mwenye kuogopesha,[p] asiyemtendea yeyote kwa upendeleo[q] wala kukubali rushwa,[r] **18** anayetekeleza haki kwa ajili ya mvulana asiye na baba na mjane[s] na kumpenda mkaaji mgeni[t] ili kumpa mkate na nguo ya kujitanda. **19** Ninyi pia lazima mumpende mkaaji mgeni,[u] kwa maana mlikuwa wakaaji wageni katika nchi ya Misri.[v]

20 "Unapaswa kumwogopa Yehova Mungu wako.[w] Unapaswa kumtumikia yeye,[x] nawe unapaswa kushikamana naye,[y] na kwa jina lake unapaswa kutoa ahadi zenye kiapo.[z] **21** Yeye ndiye unayepaswa kumsifu,[a] naye ni Mungu wako, ambaye amekutendea wewe mambo haya makuu na yenye kuogopesha ambayo macho yako yameona.[b] **22** Mababu zako walishuka kuingia Misri[c] wakiwa na nafsi 70, na sasa Yehova Mungu wako amekufanya kama nyota za mbinguni kwa wingi.[d]

11 "Nawe umpende Yehova Mungu[e] wako na kushika wajibu wako kwake na sheria zake na maamuzi yake ya hukumu[f] na amri zake sikuzote. **2** Nanyi mnajua vema leo (kwa maana mimi sihutubii wana wenu ambao hawajajua wala hawajaona nidhamu ya Yehova[g] Mungu wenu, ukuu wake,[h] mkono wake wenye nguvu[i] na mkono wake ulionyooshwa,[j] **3** wala ishara zake na matendo yake aliyotenda katikati ya Misri[k] kwa Farao mfalme wa Misri na kwa nchi yake yote; **4** wala mambo aliyotendea majeshi ya Misri, farasi zake na magari yake ya vita ambao dhidi ya nyuso zao aliyafanya maji ya Bahari Nyekundu yafurike walipokuwa wakiwafuatilia,[l] na Yehova akawaangamiza mpaka leo hii;[m] **5** wala mambo aliyowatendea ninyi nyikani mpaka mlipokuja mahali hapa; **6** wala mambo aliyowatendea Dathani na Abiramu[n] wana wa Eliabu mwana wa Rubeni, wakati dunia ilipofungua kinywa chake na kuwameza pamoja na nyumba zao na mahema yao na kila kitu kilichokuwako ambacho kilipiga hatua na kuwafuata katikati ya Israeli yote);[o] **7** kwa maana macho yenu

SURA 10

a Mwa 15:18
b Mik 6:8
c Kum 5:29 Kum 6:13 Zb 34:9 Met 8:13
d Kum 5:33 Yos 22:5 Eze 11:20
e Kum 30:16
f Kum 6:5 Kum 11:13 Lu 10:27
g Kut 24:7
h Kum 6:24
i Zb 89:11 Zb 115:16 Isa 66:1
j 1Nya 29:11 Zb 24:1 1Ko 10:26
k Kum 4:37 Zb 105:6
l Kum 30:6 Yer 4:4 Ro 2:29 Flp 3:3 Kol 2:11
m Kut 34:9 Kum 9:6 Kum 31:27
n Kut 18:11 2Nya 2:5 Zb 97:9
o Zb 136:3
p Kum 7:21 Ne 1:5 Ne 9:32
q Ayu 34:19 Mdo 10:34 Ro 2:11 Efe 6:9
r 2Nya 19:7
s Zb 68:5 Zb 146:9 Yak 1:27
t Law 19:10 Kum 24:14
u Law 19:34
v Kut 22:21
w Kum 6:13
x Lu 4:8
y Kum 13:4
z Kum 6:13

Safu ya 2

a Kut 15:2 Zb 105:45 Ufu 19:6
b 2Sa 7:23
c Mwa 46:27 Kut 1:5 Mdo 7:14
d Mwa 15:5 Kum 1:10 Ne 9:23

SURA 11

e Kum 6:5 Kum 10:12 Mk 12:30
f Kum 4:45
g Kum 8:5 Ebr 12:6
h Kum 5:24 Kum 9:26
i Kut 13:3
j Kum 7:19 Isa 63:12
k Kum 4:34 Ne 9:10 Zb 105:27

l Kut 14:23; Zb 136:15; Ebr 11:29; m Kut 14:28; Kut 15:4; n Hes 16:1; Zb 106:17; o Hes 16:32.

ndiyo yaliyoona matendo hayo
makubwa ya Yehova ambayo ali-
yatenda.[a]
8 "Nanyi mtashika amri yote
ninayowaamuru leo,[b] ili muwe
na nguvu na mpate kuingia na
kuimiliki nchi ambayo mnavu-
ka ili kuimiliki,[c] **9** na ili mre-
fushe siku zenu[d] kwenye udo-
ngo ambao Yehova aliwaapia
mababu zenu kwamba atawapa
wao na uzao wao,[e] nchi inayoti-
ririka maziwa na asali.[f]
10 "Kwa maana ile nchi una-
yoenda kuimiliki si kama nchi ya
Misri mliyotoka, mahali ambapo
ulikuwa ukipanda mbegu yako
nawe ulikuwa ukimwagilia maji
kwa mguu wako, kama busta-
ni ya mboga. **11** Lakini nchi
mnayovuka ili kuimiliki ni nchi
yenye milima na nchi tambar-
are za mabonde.[g] Inakunywa
maji ya mvua ya mbinguni;
12 nchi ambayo Yehova Mu-
ngu wako anaitunza. Macho[h]
ya Yehova Mungu wako yako
juu yake daima, toka mwanzo
wa mwaka mpaka mwisho wa
mwaka.
13 "Na itatukia kwamba iki-
wa mtatii amri[i] zangu ninazo-
waamuru ninyi leo ili kumpe-
nda Yehova Mungu wenu na
kumtumikia kwa moyo wenu
wote na kwa nafsi yenu yote,[j]
14 mimi pia nitatoa mvua kwa
ajili ya nchi yenu katika wakati
wake uliowekwa,[k] mvua ya vuli
na mvua ya masika,[l] nawe kwa
kweli utakusanya nafaka yako
na divai yako tamu na mafu-
ta yako. **15** Nami nitatokeza
majani katika shamba lako kwa
ajili ya wanyama wa kufugwa,[m]
nawe kwa kweli utakula na ku-
shiba.[n] **16** Jiangalieni mioyo
yenu isije ikashawishiwa,[o] na-
nyi mgeuke kando na kuabu-
du miungu mingine na kuiina-
mia,[a] **17** na hasira ya Yehova
iwake juu yenu, naye afunge
mbingu hivi kwamba mvua yo-
yote isitokee[b] nayo nchi isitoe
mazao yake nanyi mwangamie
haraka kutoka katika nchi nzu-
ri ambayo Yehova anawapa ni-
nyi.[c]
18 "Nanyi mtatia maneno
haya yangu katika moyo wenu[d]
na nafsi yenu na kuyafunga
kama ishara juu ya mkono
wenu, nayo yatakuwa kama
utepe wa kipaji katikati ya ma-
cho yenu.[e] **19** Pia mtawafu-
ndisha wana wenu, ili kusema
juu yake unapoketi katika nyu-
mba yako na unapotembea ba-
rabarani na unapolala na una-
poamka.[f] **20** Nawe utayaandi-
ka juu ya miimo ya mlango
wa nyumba yako na kwe-
nye malango yako,[g] **21** ili siku
zenu na siku za wana wenu ziwe
nyingi[h] juu ya nchi ambayo Ye-
hova aliwaapia mababu zenu
kwamba atawapa,[i] kama siku za
mbingu juu ya dunia.[j]
22 "Kwa maana ikiwa mtai-
shika kabisa amri yote hii[k] ni-
nayowaamuru ninyi ili kuifa-
nya, kumpenda Yehova Mungu
wenu,[l] kutembea katika njia
zake[m] na kushikamana naye,[n]
23 Yehova pia atayafukuzia
mbali mataifa yote haya kwa
sababu yenu,[o] nawe hakika uta-
yafukuza mataifa yaliyo maku-
bwa zaidi na yenye watu wengi
zaidi kuliko wewe.[p] **24** Kila
mahali ambapo wayo wa mguu
wenu utakanyaga patakuwa
penu.[q] Mpaka wenu utakuwa
kutoka nyikani hadi Lebano-
ni, kutoka ule Mto, mto Efra-
ti, hadi bahari ya magharibi.[r]

SURA 11
a Kum 7:19; Kum 29:3
b Mt 5:19
c Kum 1:38
d Kum 4:40; Zb 91:16; Met 3:2; Met 10:27
e Mwa 13:15; Mwa 26:3; Mwa 28:13; Kum 9:5
f Kut 3:8; Eze 20:6
g Kum 1:7; Kum 8:7; Kum 8:9
h 1Fa 9:3; Zb 33:18; Zb 34:15
i Kut 15:26; Kum 6:17
j Kum 4:29; Kum 6:5; Kum 10:12; Mt 22:37
k Law 26:4; Kum 28:12; Zb 65:10; Isa 30:23; Yer 14:22
l Yer 5:24; Yoe 2:23; Yak 5:7
m Zb 104:14
n Kum 6:11; Kum 8:10; Yoe 2:19
o Kum 29:18; Ayu 31:27; Ebr 3:12

Safu ya 2
a Kum 8:19; Kum 30:17
b Kum 28:23; 1Fa 8:35; 2Nya 7:13; Amo 4:7
c Kum 4:26; Kum 8:19; Kum 30:18; Yos 23:13
d Kum 6:6; Zb 37:31; Met 7:3; Isa 51:7
e Kut 13:9; Kut 13:16; Kum 6:8
f Kum 4:9; Kum 6:7; Zb 34:11; Zb 78:5; Met 22:6; Efe 6:4
g Kum 6:9
h Kum 4:40; Kum 6:2; Met 3:2; Met 4:10; Met 9:11
i Mwa 13:15
j Zb 72:5; Zb 89:29
k Kum 6:17; Kum 11:13; Mhu 12:13
l Kum 6:5; Lu 10:27
m Yos 22:5; Zb 81:13; Eze 11:20
n Kum 10:20; Kum 13:4
o Kut 23:28; Kum 9:5; Yos 3:10; Zb 44:2;
p Kum 4:38; Kum 7:1; Kum 9:1;
q Yos 1:3; Yos 14:9;
r Mwa 15:18; Kut 23:31.

25 Hakuna mtu atakayesimama imara dhidi yenu.[a] Yehova Mungu wenu atatia mbele ya uso wa nchi[b] yote ambayo mtaikanyaga hofu kwa ajili yenu na woga kwa ajili yenu kama vile alivyowaahidi ninyi.

26 "Tazama, ninaweka mbele yenu leo baraka na laana:[c] **27** baraka, ikiwa mtatii amri za Yehova Mungu[d] wenu ninazowaamuru ninyi leo; **28** na laana,[e] ikiwa hamtatii amri za Yehova Mungu[f] wenu nanyi mgeuke kutoka katika njia ambayo ninawaamuru ninyi juu yake leo, ili kufuata miungu mingine ambayo hamjaijua.

29 "Na itatukia kwamba wakati Yehova Mungu wako atakapokuleta ndani ya nchi ambayo utaimiliki,[g] utatoa pia baraka juu ya Mlima Gerizimu[h] na laana juu ya Mlima Ebali.[i] **30** Je, haiko upande wa Yordani kuelekea upande wa magharibi, katika nchi ya Wakanaani wanaokaa Araba,[j] mbele ya Gilgali,[k] kando ya ile miti mikubwa ya More?[l] **31** Kwa maana mnavuka Yordani mwingie ndani kuimiliki nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa ninyi, nanyi mtaimiliki na kukaa ndani yake.[m] **32** Nanyi muwe waangalifu ili kutimiza masharti yote na maamuzi ya hukumu[n] ninayoweka mbele yenu leo.[o]

12 "Haya ndiyo masharti[p] na maamuzi ya hukumu[q] ambayo mnapaswa kuwa waangalifu kuyatimiza[r] katika nchi ambayo Yehova Mungu wa mababu zenu atawaruhusu kuimiliki, siku zote mtakazokuwa hai kwenye nchi hiyo.[s] **2** Mnapaswa kuangamiza kabisa[a] mahali pote ambapo mataifa mnayoyafukuza yameitumikia miungu yao, juu ya milima mirefu na vilima na chini ya kila mti wenye majani mengi.[b] **3** Nanyi mtabomoa madhabahu[c] zao na kuvunja-vunja nguzo zao takatifu,[d] nanyi mtaiteketeza miti yao mitakatifu[e] katika moto na kukata sanamu za kuchongwa[f] za miungu yao, nanyi mtayaharibu majina yao kutoka mahali hapo.[g]

4 "Msimfanyie hivyo Yehova Mungu wenu,[h] **5** lakini mahali ambapo Yehova Mungu wenu atachagua kutoka katika makabila yenu yote ili kuliweka jina lake hapo, kulifanya likae, hapo ndipo mtapatafuta, nanyi mje hapo.[i] **6** Na hapo mtaleta matoleo yenu ya kuteketezwa na dhabihu[j] zenu na sehemu zenu za kumi[k] na mchango wa mkono wenu[l] na matoleo yenu ya nadhiri[m] na matoleo yenu ya hiari[n] na wazaliwa wa kwanza wa mifugo yenu na wa kundi lenu.[o] **7** Na hapo mtakula mbele za Yehova Mungu[p] wenu na kushangilia katika kazi zenu zote,[q] ninyi na nyumba zenu, kwa sababu Yehova Mungu wako amekubariki.

8 "Msifanye kulingana na mambo yote ambayo tunafanya hapa leo, kila mmoja lolote linaloonekana kuwa sawa machoni pake mwenyewe,[r] **9** kwa sababu bado hamjaingia katika mahali pa kupumzika[s] na urithi ambao Yehova Mungu wako anakupa wewe. **10** Nanyi mtavuka Yordani[t] na kukaa katika nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa iwe

SURA 11
a Kum 7:24 Yos 1:5
b Kut 23:27 Kum 2:25 Yos 2:9 Yos 5:1
c Kum 28:2 Kum 28:15 Kum 30:1 Kum 30:15
d Kum 28:1 Zb 19:11 Isa 1:19
e Law 26:16 Isa 1:20
f Ro 2:8 Ro 2:9
g Kut 23:23 Kum 9:1
h Kum 27:12 Yos 8:33
i Kum 27:13 Yos 8:34
j Kum 1:7 Kum 3:17 Yos 12:3
k 2Fa 4:38
l Mwa 12:6
m Kum 9:1 Yos 1:11
n Kum 4:45
o Kum 5:32 Kum 12:32 Zb 119:4 1Yo 5:3

SURA 12
p Law 26:46 Kum 4:5
q Law 19:37 Law 25:18
r Kum 4:40 Kum 6:1 Yak 1:22
s Kum 4:10 1Fa 8:40

Safu ya 2
a Kut 34:13
b Eze 20:28
c Amu 2:2 Amu 6:25
d Kut 23:24 2Fa 18:4
e Kut 34:13 1Fa 15:13 2Fa 23:14 2Nya 14:3
f Hes 33:52 Kum 7:5 Kum 7:25
g Kut 23:13 Yos 23:7
h Law 18:3 Kum 12:31 2Fa 17:15
i Kum 26:2 2Nya 7:12
j Law 1:3
k Kum 12:17 Kum 14:22
l Hes 18:19 Kum 12:11
m Law 7:16 Law 22:18
n Law 23:38 1Nya 29:9 Ezr 2:68
o Kum 12:17 Kum 15:19
p Kum 14:23 Kum 15:20

q Law 23:40; Kum 12:12; Kum 12:18; Kum 14:26; Zb 32:11; Zb 100:2; Flp 4:4; r Hes 15:39; Amu 17:6; Met 21:2; s 1Fa 8:56; 1Nya 23:25; Ebr 4:8; t Yos 3:17.

miliki,[a] naye atawapa pumziko
kutokana na adui zenu wanaowazunguka, nanyi hakika mtakaa kwa usalama.[b] **11** Na ita-
tukia kwamba mahali[c] ambapo
Yehova Mungu wenu atachagua
ili jina lake likae hapo ndipo
mtakapoleta vyote ambavyo ni-
nawaamuru leo, matoleo yenu
ya kuteketezwa[d] na dhabihu
zenu, na sehemu zenu za kumi[e]
na mchango[f] wa mkono wenu
na kila kilicho bora cha ma-
toleo yenu ya nadhiri[g] amba-
yo mtamwekea nadhiri Yehova.
12 Nanyi mtashangilia mbele
za Yehova Mungu wenu,[h] ninyi
na wana wenu na binti zenu
na watumishi wenu na vijaka-
zi wenu na Mlawi aliye ndani
ya malango yenu, kwa sababu
hana fungu wala urithi pamoja
nanyi.[i] **13** Jiangalie usije uka-
toa matoleo yako ya kuketete-
zwa katika mahali pengine po-
pote utakapoona.[j] **14** Bali ka-
tika mahali ambapo Yehova ata-
chagua katika moja la makabila
yako ndipo utakapotoa matoleo
yako ya kuteketezwa, na hapo
ndipo utakapofanya yote nina-
yokuamuru wewe.[k]

15 "Ila wakati wowote amba-
po nafsi yako inatamani, una-
weza kuchinja,[l] nawe utaku-
la nyama kulingana na baraka
ya Yehova Mungu wako ambayo
amekupa wewe, ndani ya mala-
ngo yako yote. Asiye safi[m]
pamoja na aliye safi watawe-
za kula, kama swala na kama
paa.[n] **16** Ila tu damu msi-
le.[o] Utaimwaga kwenye udongo
kama maji.[p] **17** Hutaruhusi-
wa kula ndani ya malango yako
sehemu ya kumi ya nafaka[q]
yako au ya divai yako mpya au
ya mafuta yako au mzaliwa wa
kwanza wa mifugo[r] yako na wa

SURA 12

a Kum 4:22
Kum 9:1
b Kum 33:28
1Fa 4:25
Zb 4:8
Met 1:33
c Kum 12:6
Kum 14:23
Kum 16:2
Kum 26:2
d Law 1:3
e Kum 14:22
Kum 26:12
f Hes 18:19
Kum 12:6
g Law 7:16
Law 22:18
h Kum 14:26
1Fa 8:66
Ne 8:10
Flp 4:4
i Hes 18:24
Kum 10:9
Kum 14:29
Yos 13:14
j Law 17:4
1Fa 12:28
k 2Nya 7:12
l Kum 12:21
Kum 14:26
m Law 5:2
Law 13:3
n Kum 14:5
Kum 15:22
o Mwa 9:4
Law 7:26
Law 17:10
Kum 15:23
1Sa 14:33
Eze 33:25
Mdo 15:29
p Law 17:13
Kum 15:23
q Kum 14:22
r Kum 12:6
Kum 14:23

Safu ya 2

a Law 23:38
b Hes 18:11
c Kum 12:11
Kum 14:23
d Kum 12:7
Kum 12:12
Flp 3:1
e Hes 18:21
Kum 14:27
2Nya 31:4
Ne 10:38
Mal 3:8
f 1Fa 4:21
g Mwa 15:18
Kut 34:24
Kum 11:24
h Law 11:2
Kum 14:4
i Kum 14:23
2Nya 7:12
j Kum 12:15
k Kum 14:5
Kum 15:22
l Law 15:3
Law 15:16
m Law 3:17
Kum 12:16
n Mwa 9:4
Law 17:11
Law 17:14
o Law 17:13
Kum 15:23
p Kum 4:40
Isa 3:10

kundi lako au yoyote ya ma-
toleo yako ya nadhiri utakayo-
weka nadhiri au matoleo yako
ya hiari[a] au mchango wa mko-
no wako.[b] **18** Lakini mbele za
Yehova Mungu wako utaila, ka-
tika mahali ambapo Yehova
Mungu wako atachagua,[c] wewe
na mwana wako na binti yako
na mtumishi wako na kijaka-
zi wako na Mlawi aliye ndani
ya malango yako; nawe utasha-
ngilia[d] mbele za Yehova Mu-
ngu wako katika kazi zako zote.
19 Jiangalie usije ukamwacha
Mlawi[e] siku zako zote kwenye
nchi yako.

20 "Wakati ambapo Yehova
Mungu wako atalipanua eneo
lako,[f] kama vile ambavyo ame-
kuahidi,[g] nawe hakika utase-
ma, 'Acha nile nyama,' kwa sa-
babu nafsi yako inatamani kula
nyama, wakati wowote ambapo
nafsi yako inatamani unaweza
kula nyama.[h] **21** Ikiwa maha-
li ambapo Yehova Mungu wako
atachagua kuweka jina lake[i]
hapo patakuwa mbali nawe, basi
utachinja sehemu ya mifugo
yako au sehemu ya kundi lako
ambalo Yehova amekupa wewe,
kama vile ambavyo nimekua-
muru wewe, nawe utakula nda-
ni ya malango yako wakati wo-
wote ambapo nafsi yako inai-
tamani.[j] **22** Kama vile tu
swala na paa huliwa, ndivyo
utakavyoila:[k] asiye safi[l] na ali-
ye safi pamoja unaweza kuila.
23 Ila tu uazimie kwa uthabiti
usile damu,[m] kwa sababu damu
ndiyo nafsi[n] nawe usile nafsi pa-
moja na nyama. **24** Usiile. Ui-
mwage kwenye udongo kama
maji.[o] **25** Usiile, ili mambo ya-
kuendee vema[p] wewe na wana
wako baada yako, kwa sababu

utafanya yaliyo sawa machoni
pa Yehova.[a] **26** Vitu vyako vi-
takatifu[b] tu ndivyo vitakavyo-
kuwa vyako, na matoleo yako
ya nadhiri[c] utayachukua, nawe
utakuja mahali ambapo Yehova
atachagua.[d] **27** Nawe utatoa
matoleo yako ya kuteketezwa,[e]
nyama na damu,[f] juu ya madha-
bahu ya Yehova Mungu wako;
na damu ya dhabihu zako itami-
minwa juu ya madhabahu ya Ye-
hova[g] Mungu wako, bali nyama
unaweza kula.

28 "Uwe mwangalifu, nawe
utii maneno yote haya amba-
yo ninakuamuru wewe,[h] ili ma-
mbo yakuendee vema[i] wewe
na wana wako baada yako
mpaka wakati usio na kipimo,
kwa sababu utafanya yaliyo
mema na sawa machoni pa Ye-
hova Mungu wako.[j]

29 "Yehova Mungu wako
atakapoyakatilia mbali kuto-
ka mbele yako mataifa amba-
yo unaenda kuyafukuza,[k] uta-
yafukuza na kukaa katika nchi
yao.[l] **30** Jiangalie usije uka-
naswa na kuwafuata,[m] baada
ya wao kuangamizwa kutoka
mbele yako, nawe usije ukauli-
za kuhusu miungu yao, na ku-
sema, 'Mataifa haya yalikuwa
yakiitumikiaje miungu yao?
Nami, naam, mimi nitafanya vi-
vyo hivyo.' **31** Usimfanyie hi-
vyo Yehova Mungu wako,[n] kwa
maana kila kitu kinachochuki-
za kwa Yehova, ambacho ana-
chukia wameifanyia miungu
yao, kwa maana hata wana wao
na binti zao wao huwatekete-
za motoni kwa ukawaida kwa
ajili ya miungu yao.[o] **32** Kila
neno ninalowaamuru ninyi ndi-
lo mtakalokuwa waangalifu ku-
lifanya.[p] Msiongeze juu yake
wala kuondoa kutoka kwake.[q]

SURA 12

a Kum 6:18
Kum 13:18
b Hes 5:9
Hes 18:19
c Law 22:18
d Kum 12:11
e Law 1:9
f Law 17:11
g Law 4:30
h Zb 89:31
Zb 105:45
1Yo 5:3
i Ga 6:7
j Met 4:4
k Kut 23:23
Kum 9:3
Kum 19:1
Zb 44:2
Zb 78:55
l Kum 6:10
Zb 105:44
m Kum 7:16
Zb 106:36
Eze 20:28
Efe 4:17
n Law 18:3
Kum 12:4
o Law 18:21
Law 20:2
Kum 18:10
2Fa 17:15
Yer 32:35
p Kum 5:1
Yos 22:5
Zb 119:4
q Kum 4:2
Yos 1:7
Met 30:6

Safu ya 2

SURA 13

a Kum 18:22
Yer 6:13
Eze 13:2
Zek 13:4
b Yer 23:25
Yer 27:9
c Mk 13:22
2Th 2:9
d Yer 28:9
Mt 7:22
e Isa 8:19
f Kum 8:2
Zb 66:10
Mt 24:24
1Ko 11:19
2Th 2:11
g Kum 6:5
Kum 10:12
Mt 22:37
h Kum 10:20
i Isa 9:15
j Kum 18:20
Yer 14:14
Zek 13:3
k Kum 6:14
l Kum 17:7
1Ko 5:13
m 1Sa 18:1
n 1Fa 11:4
2Pe 2:1

13 "Ikiwa nabii[a] au mwotaji
wa ndoto[b] atainuka kati-
kati yenu naye awape ishara au
kitu cha ajabu,[c] **2** nayo isha-
ra hiyo au kitu hicho cha aja-
bu kiwe kweli alichokuambia,[d]
akisema, 'Na tuifuate miungu
mingine, ambayo wewe hukui-
jua, nasi tuitumikie,' **3** usisi-
kilize maneno ya nabii huyo au
mwotaji huyo wa ndoto,[e] kwa
sababu Yehova Mungu wenu
anawajaribu[f] apate kujua ikiwa
ninyi mnampenda Yehova Mu-
ngu wenu kwa moyo wenu
wote na kwa nafsi yenu yote.[g]
4 Mnapaswa kumfuata Yeho-
va Mungu wenu, nanyi mna-
paswa kumwogopa yeye, na-
nyi mnapaswa kuzishika amri
zake, nanyi mnapaswa kuisi-
kiliza sauti yake, nanyi mna-
paswa kumtumikia yeye, na-
nyi mnapaswa kushikamana
naye.[h] **5** Na nabii[i] huyo au
mwotaji huyo wa ndoto ataua-
wa,[j] kwa sababu amesema maa-
si juu ya Yehova Mungu wenu,
ambaye aliwatoa ninyi katika
nchi ya Misri na amekukomboa
kutoka katika nyumba ya watu-
mwa, ili kukugeuza kutoka ka-
tika njia ambayo Yehova Mu-
ngu wako amekuamuru kuite-
mbea;[k] nawe utaondolea mba-
li kilicho kiovu kutoka katikati
yako.[l]

6 "Ikiwa ndugu yako, mwa-
na wa mama yako, au mwa-
na wako au binti yako au mke
wako mpendwa au mwenza-
ko aliye kama nafsi yako mwe-
nyewe,[m] atajaribu kukushawi-
shi kwa siri, akisema, 'Twende
tukaitumikie miungu mingi-
ne,'[n] ambayo hukuijua, wewe
wala mababu zako, **7** baadhi
ya miungu ya watu wanaowa-
zunguka ninyi pande zote, wale

walio karibu nawe au wale walio mbali nawe, kutoka mwisho mmoja wa nchi mpaka mwisho mwingine wa nchi, **8** usikubali nia yake wala kumsikiliza,[a] wala jicho lako lisimsikitikie,[b] wala usione huruma, wala kumficha kwa kumlinda; **9** bali lazima umuue.[c] Mkono wako utakuwa wa kwanza kuja juu yake ili kumuua, nao mkono wa watu wote baadaye.[d] **10** Nawe utampiga kwa mawe, naye atakufa,[e] kwa sababu alijaribu kukugeuza mbali na Yehova Mungu wako, ambaye amekutoa katika nchi ya Misri, kutoka katika nyumba ya watumwa.[f] **11** Ndipo Israeli wote watasikia na kuogopa, nao hawatafanya tena jambo lolote kama jambo hilo baya kati yako.[g]

12 "Ikiwa utasikia ikisemwa katika moja la majiji yako, ambayo Yehova Mungu wako anakupa ukae humo, **13** 'Watu wasiofaa kitu wametokea katikati yako[h] ili wajaribu kuwageuzia mbali wakaaji wa jiji lao,[i] kwa kusema: "Twende tukaitumikie miungu mingine," ambayo hamjaijua,' **14** mtatafuta na kupeleleza na kuuliza habari kabisa;[j] na ikiwa jambo hili limethibitika kuwa kweli, jambo hilo lenye kuchukiza limefanywa katikati yako, **15** lazima utawapiga wakaaji wa jiji hilo kwa makali ya upanga.[k] Uliharibu[l] pamoja na kila kitu kilicho ndani yake, na wanyama wake wa kufugwa kwa makali ya upanga. **16** Na nyara zake zote utakusanya katikati ya kiwanja chake cha watu wote, nawe utaliteketeza jiji[m] hilo kwa moto pamoja na nyara zake zote kama toleo zima la kuteketezwa kwa Yehova Mungu wako, nalo litakuwa rundo la mabomoko mpaka wakati usio na kipimo.[a] Halipaswi kujengwa tena kamwe. **17** Na kitu chochote kisishikamane na mkono wako kutoka katika kitu kilichofanywa kuwa kitakatifu kwa marufuku,[b] ili Yehova ageukie mbali kutoka kwa hasira yake inayowaka[c] naye awape ninyi rehema,[d] naye awaonyeshe rehema na kuwazidisha, kama vile alivyowaapia mababu zenu.[e] **18** Kwa maana unapaswa kuisikiliza sauti ya Yehova Mungu wako kwa kushika amri[f] zake zote ambazo ninakuamuru leo, ili kufanya yaliyo sawa machoni pa Yehova Mungu wako.[g]

14 "Ninyi ni wana wa Yehova Mungu wenu.[h] Msijikatekate[i] wala kujitia upara[j] kwenye mapaji ya nyuso zenu kwa ajili ya mtu aliyekufa. **2** Kwa maana ninyi ni watu watakatifu[k] kwa Yehova Mungu wenu, naye Yehova amewachagua ninyi muwe watu wake, mali ya pekee,[l] kutoka kati ya vikundi vyote vya watu vilivyo kwenye uso wa nchi.

3 "Usile kitu chenye kuchukiza cha namna yoyote.[m] **4** Hii ndiyo aina ya wanyama mnaoweza kula:[n] ng'ombe, kondoo na mbuzi, **5** paa[o] na swala na kulungu na mbuzi-mwitu na palahala na kondoo-mwitu na paa-mbuzi; **6** na kila mnyama mwenye ukwato uliopasuka na ambaye ana mpasuko kwenye kwato mbili, mnyama anayecheua kati ya wanyama.[p] Huyo mnaweza kumla. **7** Aina hii tu ndiyo ambayo hampaswi kula kati ya wale wanaocheua au wenye ukwato uli-

SURA 13

a Met 1:10; Ga 1:8
b Eze 9:5
c Kut 22:20; Kut 32:27; Hes 25:5
d Kum 17:7
e Law 20:2; Law 20:27; Kum 17:5
f Kut 13:3
g Kum 17:13; Kum 19:20; 1Ti 1:20; 1Ti 5:20
h 1Sa 2:12; 1Fa 21:10; Yud 19
i 2Fa 17:21
j Kum 17:4; Kum 19:15; 1Ti 5:19; Ebr 10:28
k 2Nya 28:6
l Kut 22:20; Law 27:28
m Yos 6:24

Safu ya 2

a Yos 8:28; Yer 49:2; Mik 1:6
b Yos 6:18; Yos 7:1
c Yos 7:26; Yos 22:20
d Kut 33:19; Zb 78:38
e Mwa 22:17; Mwa 26:4; Mwa 28:14
f Kum 12:32; Ne 1:5; Zb 119:4; 1Yo 5:3
g Kut 15:26; Kum 6:18

SURA 14

h Isa 63:16; Isa 64:8; Yer 3:19; 1Ko 8:6
i Law 19:28; Yer 16:6
j Law 21:5
k Kut 19:6; Law 19:2; Law 20:26; Kum 28:9; Ezr 9:2; 1Pe 1:15
l Kut 19:5; Kum 7:6; Kum 26:18
m Law 11:43; Law 20:25; Eze 4:14; Mdo 10:14
n Law 11:2
o 1Fa 4:23
p Law 11:3

opasuka, wenye mwatuko: ngamia[a] na sungura[b] na wibari,[c] kwa sababu hao hucheua lakini hawana ukwato uliopasuka. Hao si safi kwenu. **8** Nguruwe[d] pia, kwa sababu ana ukwato uliopasuka lakini hacheui. Huyo si safi kwenu. Msile yoyote ya nyama yao, na mizoga yao msiiguse.[e]

9 "Aina hii kutoka kati ya kila kitu kilicho majini mnaweza kula: Kila kitu chenye mapezi na magamba mnaweza kula.[f] **10** Na kila kitu ambacho hakina mapezi wala magamba msile.[g] Hicho si safi kwenu.

11 "Ndege yeyote aliye safi mnaweza kula. **12** Lakini hawa ndio ndege ambao hampaswi kuwala: tai na furukombe na tai-mzoga mweusi,[h] **13** na mwewe mwekundu na mwewe mweusi[i] na ndegembua kulingana na aina yake; **14** na kila kunguru[j] kulingana na aina yake; **15** na mbuni[k] na bundi na shakwe na kipanga kulingana na aina yake; **16** na bundi mdogo na bundi mwenye masikio marefu[l] na bata-maji, **17** na mwari[m] na tai-mzoga na mnandi, **18** na korongo na kulastara kulingana na aina yake, na hudihudi na popo.[n] **19** Na kila kiumbe kinachozaana kwa wingi chenye mabawa si safi kwenu.[o] Havipaswi kuliwa. **20** Kiumbe chochote safi kinachoruka mnaweza kula.

21 "Msile mwili wowote uliokufa tayari.[p] Mkaaji mgeni aliye ndani ya malango yako unaweza kumpa mwili huo, naye ataula; au mwili huo unaweza kuuziwa mgeni, kwa sababu wewe ni kikundi cha watu watakatifu kwa Yehova Mungu wako.

SURA 14

a Law 11:4
b Law 11:6
c Law 11:5
d Law 11:7
Isa 65:4
Isa 66:17
e Law 11:8
f Law 11:9
g Law 11:10
h Law 11:13
i Law 11:14
j Law 11:15
k Law 11:16
l Law 11:17
m Law 11:18
n Law 11:19
o Law 11:20
p Kut 22:31
Law 17:15
Law 22:8
Eze 4:14

Safu ya 2

a Kut 23:19
Kut 34:26
b Kum 12:11
Kum 26:12
c Kum 12:6
d Kum 12:17
Kum 15:19
e Zb 5:7
Zb 19:9
Zb 111:10
Met 8:13
Isa 8:13
Ebr 12:28
f Kut 23:31
Kum 11:24
Kum 12:21
g Kum 12:5
h Kut 23:25
Kum 28:5
Met 10:22
Mal 3:10
i Kum 12:15
j Hes 28:7
k Kum 12:7
Kum 26:11
Zb 100:2
l Hes 18:21
Kum 12:19
2Nya 31:4
1Ko 9:13
m Hes 18:20
Hes 26:62
Kum 10:9
Yos 14:3
n Kum 26:12
o Kum 12:12

"Usimtokose mwana-mbuzi katika maziwa ya mama yake.[a]

22 "Lazima utatoa sehemu ya kumi ya mazao yako yote ya mbegu yako, yanayotoka shambani mwaka baada ya mwaka.[b] **23** Na mbele za Yehova Mungu wako, katika mahali ambapo atachagua ili jina lake likae hapo, utakula sehemu ya kumi ya nafaka yako,[c] divai yako mpya na mafuta yako na wazaliwa wa kwanza wa mifugo yako na wa kundi lako;[d] ili ujifunze kumwogopa Yehova Mungu wako sikuzote.[e]

24 "Sasa ikiwa safari itakuwa ndefu mno kwako,[f] kwa sababu hutaweza kuichukua, kwa kuwa mahali ambapo Yehova Mungu wako atachagua kuweka jina lake[g] patakuwa mbali mno nawe, (kwa sababu Yehova Mungu wako atakubariki,)[h] **25** basi utaigeuza kuwa pesa, nawe utafunga pesa hizo katika mkono wako na kusafiri mpaka mahali ambapo Yehova Mungu wako atapachagua. **26** Nawe utatoa pesa hizo kwa ajili ya chochote ambacho nafsi yako itatamani[i] kati ya ng'ombe na kondoo na mbuzi na divai na kileo[j] na kitu chochote ambacho huenda nafsi yako ikakuomba; nawe utakula huko mbele za Yehova Mungu wako na kushangilia,[k] wewe na nyumba yako. **27** Na Mlawi aliye ndani ya malango yako, hutamwacha,[l] kwa maana yeye hana fungu wala urithi pamoja nawe.[m]

28 "Mwishoni mwa miaka mitatu utatoa sehemu yote ya kumi ya mazao yako ya mwaka huo,[n] nawe utaiweka ndani ya malango yako. **29** Naye Mlawi,[o] kwa sababu hana fungu

wala urithi pamoja nawe, na mkaaji mgeni[a] na mvulana asiye na baba na mjane,[b] walio ndani ya malango yako, watakuja, nao watakula na kujishibisha; ili Yehova Mungu wako apate kukubariki[c] katika kila tendo[d] la mkono wako ambalo utafanya.

15 "Mwishoni mwa kila miaka saba mtaachilia huru. **2** Nayo hii ndiyo namna ya kuachilia huru:[e] kila mkopeshaji ataachilia huru deni ambalo amemkopesha mwenzake. Hatamkaza mwenzake au ndugu yake afanye malipo,[f] kwa sababu kuachilia huru kwa ajili ya Yehova lazima kutangazwe.[g] **3** Mgeni[h] unaweza kumkaza afanye malipo; lakini chochote kilicho chako kitakachokuwa na ndugu yako, mkono wako na ukiachilie huru. **4** Hata hivyo, mtu yeyote asije kuwa maskini katikati yako, kwa sababu hakika Yehova atakubariki[i] katika nchi ambayo Yehova Mungu wako anakupa iwe urithi, uimiliki,[j] **5** ikiwa tu hutakosa kuisikiliza sauti ya Yehova Mungu wako nawe uwe mwangalifu kufanya amri yote hii ninayokuamuru leo.[k] **6** Kwa maana hakika Yehova Mungu wako atakubariki kama vile alivyokuahidi, nawe utayakopesha[l] mataifa mengi kwa rehani, lakini wewe mwenyewe hutakopa; nawe utatawala juu ya mataifa mengi, lakini hayo hayatatawala juu yako.[m]

7 "Ikiwa mmoja wa ndugu zako atakuwa maskini kati yako katika moja la majiji yako, katika nchi yako ambayo Yehova Mungu wako anakupa, usiufanye moyo wako kuwa mgumu wala kuufunga mkono wako kumwelekea ndugu yako aliye maskini.[a] **8** Kwa maana unapaswa kumfungulia mkono kwa ukarimu[b] nawe umkopeshe kwa rehani kwa kadiri anayohitaji, kile anachopungukiwa. **9** Jiangalie neno baya lisije likawa moyoni mwako,[c] na kusema, 'Mwaka wa saba, mwaka wa kuachilia huru, umekaribia,'[d] nalo jicho lako likose ukarimu kumwelekea ndugu yako aliye maskini,[e] nawe usimpe chochote, naye amlilie Yehova juu yako,[f] nayo iwe dhambi kwako.[g] **10** Unapaswa kumpa hata iweje,[h] nao moyo wako usiwe mchoyo unapompa, maana kwa sababu hiyo Yehova Mungu wako atakubariki katika kila tendo lako na katika kila kazi unayofanya.[i] **11** Kwa maana maskini hatakosa kamwe kuwako katika nchi.[j] Ndiyo sababu ninakuamuru, na kusema, 'Unapaswa kuufungua mkono wako kwa ukarimu kwa ndugu yako anayeteseka na aliye maskini katika nchi yako.'[k]

12 "Ikiwa utauziwa ndugu yako, mwanamume Mwebrania au mwanamke Mwebrania,[l] naye amekutumikia kwa miaka sita, basi katika mwaka wa saba utamruhusu aondoke kwako kama mtu aliyewekwa huru.[m] **13** Na ikiwa utamruhusu aondoke kwako kama mtu aliyewekwa huru, usimwache aondoke mikono mitupu.[n] **14** Usikose kumtayarishia kitu fulani kutoka katika kundi lako na uwanja wako wa kupuria na mafuta yako na shinikizo lako la divai. Kama vile ambavyo Yehova Mungu wako amekubariki, unapaswa ku-

SURA 14
a Kut 22:21; Kum 10:18
b Kum 26:12; Yak 1:27
c Kum 15:10; Zb 41:1; Mal 3:10
d Met 11:24; Met 19:17; Lu 6:35

SURA 15
e Law 25:2
f Yak 2:13
g Kum 31:10
h Kut 12:43; Kum 14:21; Kum 23:20
i Kum 14:29; Kum 28:8; Met 11:25; Met 14:21; Met 28:27
j Hes 33:53; Zb 135:12
k Kum 4:40; Yos 1:7; Isa 1:19
l Kum 28:12; Met 22:7
m Kum 28:13; 1Fa 4:24

Safu ya 2
a Met 21:13; Yak 2:16; 1Yo 3:17
b Law 25:35; Zb 37:26; Met 19:17; Mt 5:42; Lu 6:35; Ga 2:10
c Met 4:23; Yer 17:10; Mt 15:19
d Kum 15:1
e Met 28:22; 1Pe 4:9
f Kut 22:23; Kum 24:15; Ayu 34:28; Met 21:13; Yak 5:4
g Mt 25:45; Yak 4:17
h Mdo 20:35; 2Ko 9:7; 1Ti 6:18; Ebr 13:16
i Kum 15:4; Kum 24:19; Zb 41:1; Met 22:9; Isa 32:8; 2Ko 9:8
j Mt 26:11
k Met 3:27; Mt 5:42; Lu 12:33; Mdo 2:45
l Kut 21:2; Law 25:39
m Kum 15:1; Yer 34:14
n Kut 3:21; Kut 12:36; Met 3:27; Kol 4:1

mpa vivyo hivyo.[a] **15** Nawe ukumbuke kwamba ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri na Yehova Mungu wako alikukomboa.[b] Ndiyo sababu ninakuamuru jambo hili leo.

16 "Na itatukia kwamba ikiwa atakuambia, 'Sitakuacha!' kwa sababu anakupenda wewe na nyumba yako, kwa maana mambo yalikuwa yakimwendea vema alipokuwa pamoja nawe,[c] **17** utachukua msumari na kuupenyeza kwenye sikio lake na kwenye mlango, naye atakuwa mtumwa wako mpaka wakati usio na kipimo.[d] Nawe utamfanyia kijakazi wako vivyo hivyo. **18** Lisiwe jambo gumu machoni pako unapomruhusu aondoke katika ushirika wako akiwa mtu aliyewekwa huru;[e] kwa sababu kwa thamani mara mbili ya mfanyakazi wa kukodiwa[f] alikutumikia kwa miaka sita, na Yehova Mungu wako amekubariki katika kila kitu ambacho ulikuwa ukifanya.[g]

19 "Kila mwanamume mzaliwa wa kwanza atakayezaliwa katika mifugo yako na katika kundi lako utamtakasa kwa Yehova Mungu wako.[h] Usifanye utumishi wowote na mzaliwa wa kwanza wa ng'ombedume wako, wala kukata manyoya ya mzaliwa wa kwanza wa kundi lako.[i] **20** Utamla mbele za Yehova Mungu wako mwaka baada ya mwaka katika mahali ambapo Yehova Mungu wako atapachagua,[j] wewe na nyumba yako. **21** Na ikiwa atakuwa na kasoro, awe kilema au kipofu, kasoro yoyote mbaya, usimtoe dhabihu kwa Yehova Mungu wako.[k] **22** Ndani ya malango yako utamla, asiye safi na aliye safi pamoja,[a] kama yule swala na kama yule paa.[b] **23** Ila tu usile damu.[c] Utaimwaga kwenye udongo kama maji.[d]

16 "Mwezi wa Abibu[e] na uadhimishwe, nawe utasherehekea pasaka kwa Yehova Mungu wako,[f] kwa sababu katika mwezi wa Abibu Yehova Mungu wako alikutoa Misri wakati wa usiku.[g] **2** Nawe utatoa dhabihu ya pasaka kwa Yehova Mungu wako,[h] mnyama wa kundi na wa mifugo,[i] katika mahali ambapo Yehova atapachagua kuweka jina lake.[j] **3** Usile chochote chenye chachu pamoja nayo kwa siku saba.[k] Utakula pamoja nayo keki zisizo na chachu, mkate wa mateso, kwa sababu ulitoka katika nchi ya Misri kwa haraka,[l] ili ukumbuke siku ya kutoka kwako katika nchi ya Misri siku zote za maisha yako.[m] **4** Na unga wowote uliokandwa wenye chachu usionekane pamoja nawe katika eneo lako lote kwa siku saba,[n] wala nyama yoyote, ambayo utaitoa dhabihu katika jioni ya siku ya kwanza, isikae usiku kucha mpaka asubuhi.[o] **5** Hutaruhusiwa kutoa dhabihu ya pasaka katika lolote la majiji yako ambayo Yehova anakupa wewe. **6** Bali mahali ambapo Yehova Mungu wako atapachagua ili jina lake likae,[p] hapo utatoa dhabihu ya pasaka wakati wa jioni mara tu baada ya jua kutua,[q] wakati uliowekwa wa kutoka kwenu Misri. **7** Nanyi mtapika na kula[r] katika mahali ambapo Yehova Mungu wenu atapachagua,[s] na wakati wa asubuhi mtageuka na kwenda kwenye mahema yenu. **8** Siku sita mtakula keki zisizo

SURA 15
a Met 10:22; Mdo 20:35
b Kut 20:2; Kum 5:15; Mt 18:33
c Kut 21:5
d Kut 21:6
e Kum 15:10
f Law 19:13; Kum 24:15
g Mwa 30:30
h Kut 13:2; Kut 34:19; Law 27:26; Hes 3:13; Hes 18:15; Hes 18:17
i Kut 22:30; Kum 12:6
j Kum 12:5; Kum 14:23; Kum 16:11
k Law 22:20; Kum 17:1; Mal 1:8; Ebr 9:14

Safu ya 2
a Kum 12:15; Kum 12:22
b Kum 14:5; 1Fa 4:23
c Mwa 9:4; Law 7:26; Law 17:10; 1Sa 14:33; Mdo 15:20
d Law 17:13; Kum 12:16

SURA 16
e Kut 12:2; Kut 13:4
f Kut 12:14; Law 23:5; Hes 9:2; Hes 28:16; 1Ko 5:7; Ebr 11:28
g Kut 34:18
h Mt 26:17; Lu 22:7
i Kut 12:5; 2Nya 35:7
j Kum 12:5; 1Fa 8:29
k Kut 13:3; Law 23:6; Hes 28:17; 1Ko 5:8
l Kut 12:33
m Kut 12:14; Kut 13:8; Kut 13:9
n Kut 12:15; Kut 13:7
o Kut 12:10; Kut 34:25
p Kum 16:2
q Kut 12:6; Hes 9:3; Mt 26:20
r Kut 12:8; 2Nya 35:13
s 2Fa 23:23; Yoh 2:13; Yoh 11:55

na chachu; na siku ya saba kutakuwako kusanyiko kuu kwa Yehova Mungu wenu.[a] Hamtafanya kazi yoyote.

9 "Mtajihesabia majuma saba. Tangu wakati ambapo mundu unawekwa kwa mara ya kwanza kwenye nafaka inayosimama utaanza kuhesabu majuma saba.[b] **10** Halafu utasherehekea sherehe ya majuma kwa Yehova Mungu wako,[c] kulingana na toleo la hiari la mkono wako ambalo utatoa, kama vile Yehova Mungu wako atakavyokuwa amekubariki.[d] **11** Nawe utashangilia mbele za Yehova Mungu wako,[e] wewe na mwana wako na binti yako na mtumishi wako na kijakazi wako na Mlawi aliye ndani ya malango yako na mkaaji mgeni[f] na mvulana asiye na baba[g] na mjane,[h] walio katikati yako, katika mahali ambapo Yehova Mungu wako atapachagua ili jina lake likae.[i] **12** Nawe utakumbuka kwamba ulikuwa mtumwa katika Misri,[j] nawe utashika na kutimiza masharti haya.[k]

13 "Sherehe ya vibanda[l] utaisherehekea kwa ajili yako mwenyewe kwa siku saba wakati ambapo unakusanya kutoka katika uwanja wako wa kupuria na mafuta yako na shinikizo la divai. **14** Nawe utashangilia wakati wa sherehe yako,[m] wewe na mwana wako na binti yako na mtumishi wako na kijakazi wako na Mlawi na mkaaji mgeni na mvulana asiye na baba na mjane, walio ndani ya malango yako. **15** Siku saba utamfanyia Yehova Mungu wako sherehe[n] katika mahali ambapo Yehova atapachagua, kwa sababu Yehova Mungu wako atakubariki[o] katika mazao yako yote na katika kila tendo la mkono wako, nawe utakuwa na shangwe kwelikweli.[a]

16 "Mara tatu katika mwaka kila mwanamume wa kwako ataonekana mbele za Yehova Mungu wako katika mahali ambapo atapachagua:[b] katika sherehe ya keki zisizo na chachu[c] na katika sherehe ya majuma[d] na katika sherehe ya vibanda,[e] na mtu yeyote asionekane mbele za Yehova mikono mitupu.[f] **17** Zawadi ya mkono wa kila mtu itakuwa kulingana na baraka za Yehova Mungu wako ambazo amekupa wewe.[g]

18 "Utaweka waamuzi[h] na maofisa[i] kwa ajili yako ndani ya malango yote ambayo Yehova Mungu wako anakupa wewe kulingana na makabila yako, nao watawahukumu watu kwa hukumu ya uadilifu. **19** Usipotoshe hukumu.[j] Usipendelee[k] wala kukubali rushwa, kwa maana rushwa hupofusha macho ya wenye hekima[l] na hupotoa maneno ya waadilifu. **20** Haki—haki utaifuatilia,[m] ili upate kuendelea kuwa hai nawe umiliki nchi ambayo Yehova Mungu wako anakupa wewe.[n]

21 "Usijipandie aina yoyote ya mti ili uwe mti mtakatifu karibu na madhabahu ya Yehova Mungu wako ambayo utajifanyia.[o]

22 "Wala usijisimamishie nguzo takatifu,[p] kitu ambacho Yehova Mungu wako anakichukia kwelikweli.[q]

17 "Usimtolee Yehova Mungu wako dhabihu ya ng'ombe-dume au kondoo mwenye kasoro, kitu chochote kiba-

SURA 16

a Kut 12:16
Law 23:8
b Kut 23:16
Kut 34:22
Law 23:15
c Hes 28:26
2Nya 8:13
d Kum 16:17
1Ko 16:2
2Ko 8:12
e Kum 12:7
f Hes 15:16
g Kum 10:18
h Yak 1:27
i Kum 12:5
j Mwa 15:13
Kut 3:7
Kum 5:15
k Mhu 12:13
1Yo 5:3
l Kut 23:16
Law 23:34
Hes 29:12
Kum 31:10
Zek 14:16
Yoh 7:2
m Law 23:40
Kum 12:12
Kum 26:11
Ne 8:10
Ne 8:17
Mhu 5:18
n Law 23:36
Ne 8:18
o Kum 7:13
Kum 28:8
Kum 30:16

Safu ya 2

a Flp 4:4
1Th 5:16
b Kut 23:14
Kut 34:23
c Kut 23:15
Law 23:6
Hes 28:17
d Kum 16:10
e Kum 16:13
f Kut 23:15
Kut 34:20
Zb 96:8
g Kum 16:10
2Ko 8:12
h Kut 18:26
Kum 1:16
2Nya 19:5
i Hes 11:16
1Nya 23:4
j Kut 23:2
Law 19:15
1Sa 8:3
k Kum 1:17
Met 24:23
Mdo 10:34
l Kut 23:8
1Sa 12:3
Mhu 7:7
Amo 5:12
m Kum 25:16
Eze 18:8
Mik 6:8
n Kum 4:1
o Kut 34:13
Amu 3:7
2Nya 33:3
p Kut 23:24
Law 26:1
Kum 12:3
q Kum 12:31
Yer 44:4

ya; kwa sababu ni chukizo kwa
Yehova Mungu wako.[a]
2 "Ikiwa atapatikana katika-
ti yako katika moja la maji-
ji yako ambayo Yehova Mungu
wako anakupa wewe, mwana-
mume au mwanamke atakaye-
kuwa na mazoea ya kufanya ma-
baya machoni pa Yehova Mungu
wako na kuvunja agano lake,[b]
3 naye aende na kuabudu miu-
ngu mingine na kuinamia hiyo
au jua au mwezi au jeshi lote
la mbinguni,[c] jambo ambalo si-
jaamuru,[d] **4** nawe umeambi-
wa, ukasikia, ukatafuta kabisa,
na, tazama! jambo hilo limethibi-
tishwa kuwa kweli,[e] jambo hilo
lenye kuchukiza limefanywa
katika Israeli! **5** utamtoa nje
ya malango yako mwanamume
huyo au mwanamke huyo amba-
ye amefanya jambo hilo baya,
naam, mwanamume huyo au
mwanamke huyo, nawe uta-
mpiga kwa mawe mtu huyo,
naye lazima afe.[f] **6** Kwa ki-
nywa cha mashahidi wawili au
cha mashahidi watatu[g] anaye-
kufa atauawa. Hatauawa kwa
kinywa cha shahidi mmoja.[h]
7 Mkono wa mashahidi kwa-
nza kabisa unapaswa kuja juu
yake ili kumuua, na mkono wa
watu wote baadaye;[i] nawe uta-
kiondolea mbali kilicho kibaya
kutoka katikati yako.[j]
8 "Ikiwa jambo la uamuzi wa
hukumu litakuwa lisilo la ka-
waida kwako,[k] ambamo damu
imemwagwa,[l] ambamo dai ha-
lali limezushwa,[m] au tendo le-
nye jeuri limefanywa, mambo
ya mzozo,[n] ndani ya malango
yako, utaondoka pia na kwe-
nda mahali ambapo Yehova
Mungu wako atapachagua,[o]
9 nawe utaenda kwa makuha-
ni[p] Walawi, na kwa mwamu-
zi[a] atakayekuwa akitenda siku
hizo, nawe utauliza, nao watuku-
pa neno la uamuzi wa hukumu.[b]
10 Kisha utafanya kulingana na
lile neno watakalokupa kuto-
ka mahali hapo ambapo Yehova
atachagua; nawe utakuwa mwa-
ngalifu kufanya kulingana na
yote watakayokuagiza. **11** Ku-
lingana na sheria watakayo-
kuonyesha, na kulingana na
uamuzi wa hukumu watakaoku-
ambia, unapaswa kufanya.[c] Usi-
geuke kando ya neno watakalo-
kupa, upande wa kuume au upa-
nde wa kushoto.[d] **12** Na mtu
atakayejiendesha kwa kimbele-
mbele kwa kutomsikiliza ku-
hani anayesimama ili kuhudumu
hapo kwa Yehova Mungu wako
au kwa mwamuzi,[e] mtu huyo la-
zima afe;[f] nawe utaondolea mba-
li kilicho kibaya kutoka Israeli.[g]
13 Nao watu wote watasikia na
kuogopa,[h] nao hawatatenda kwa
kimbelembele tena.
14 "Mwishowe utakapoingia
katika nchi ambayo Yehova Mu-
ngu wako anakupa wewe, nawe
uwe umeimiliki na kukaa ndani
yake,[i] nawe uwe umesee-
ma, 'Acha niweke mfalme juu
yangu kama mataifa yote
yanayonizunguka';[j] **15** utawe-
ka juu yako mfalme ambaye
Yehova Mungu wako atacha-
gua.[k] Kutoka katikati ya ndu-
gu zako utaweka mfalme juu
yako. Hutaruhusiwa kuweka
juu yako mgeni ambaye si ndu-
gu yako. **16** Ila tu asiongeze
farasi kwa ajili yake,[l] wala ku-
wafanya watu warudi Misri ili
kuongeza farasi;[m] huku Yeho-
va amewaambia ninyi, 'Msiru-
di kamwe tena katika njia hii.'
17 Pia asizidishe wake kwa aji-
li yake, ili moyo wake usigeuke
kando;[n] wala asijiongezee sana

SURA 17
a Law 22:20
Kum 15:21
Mal 1:8
b Kum 4:23
Kum 13:6
Amu 2:20
c Kum 4:19
Yer 8:2
Eze 8:16
d Yer 7:18
Yer 19:5
e Kum 13:14
Yoh 7:51
f Kum 13:10
g Hes 35:30
Mt 18:16
Yoh 8:17
2Ko 13:1
1Ti 5:19
Ebr 10:28
h Kum 19:15
i Kum 13:9
j Kum 13:5
1Ko 5:13
k Kum 1:17
l Hes 35:11
m 1Fa 3:28
Isa 1:17
Yer 5:28
n 1Fa 3:16
o Kum 12:5
Zb 122:2
Zb 122:5
p Kum 19:17
Kum 21:5
Hag 2:11
Mal 2:7

Safu ya 2
a 1Sa 7:16
b Kum 19:17
Kum 21:5
c Mal 2:7
d Kum 5:32
Kum 12:32
Yos 1:7
Met 4:27
e Zb 19:13
Met 11:2
Ho 4:4
f Ebr 10:28
g Kum 13:5
1Ko 5:13
h Hes 15:31
Kum 13:11
Kum 19:20
i Kum 7:1
Yos 1:3
Zb 44:2
j 1Sa 8:5
1Sa 8:20
1Sa 10:19
k 1Sa 9:17
1Sa 10:24
1Sa 16:12
l Kum 20:1
2Sa 8:4
Zb 20:7
Met 21:31
m Isa 31:1
Isa 36:9
Eze 17:15
n 1Fa 11:3
Ne 13:26

fedha na dhahabu.[a] **18** Na itatukia kwamba atakapoketi kwenye kiti chake cha ufalme, atajiandikia katika kitabu nakala ya sheria hii kutoka katika ile iliyo mkononi mwa makuhani Walawi.[b]

19 "Naye atakaa nacho, na kukisoma siku zote za maisha yake,[c] kusudi ajifunze kumwogopa Yehova Mungu wake ili apate kushika maneno yote ya sheria hii na masharti haya kwa kuyafanya;[d] **20** ili moyo wake usijiinue juu ya ndugu zake[e] naye asigeuke kando kutoka kwenye amri kwenda upande wa kuume au upande wa kushoto,[f] ili arefushe siku zake juu ya ufalme wake,[g] yeye na wanawe katikati ya Israeli.

18 "Hakuna fungu au urithi pamoja na Israeli litakalokuja kuwa la makuhani, Walawi,[h] kabila zima la Lawi. Matoleo yanayotolewa kwa njia ya moto kwa Yehova, naam, urithi wake, watayala.[i] **2** Kwa hiyo hakuna urithi utakaokuja kuwa wake katikati ya ndugu zake. Yehova ndiye urithi wake,[j] kama vile alivyosema naye.

3 "Sasa hii itaendelea kuwa haki wanayostahili makuhani kutoka kwa watu, kutoka kwa wale wanaotoa dhabihu, iwe ni ng'ombe-dume au kondoo: Mtu atampa kuhani mfupa wa bega na mataya na tumbo. **4** Sehemu ya kwanza ya nafaka yako, divai yako mpya na mafuta yako na sufu yako ya kwanza iliyokatwa ya kundi lako unapaswa kumpa.[k] **5** Kwa maana yeye ndiye ambaye Yehova Mungu wako amechagua kutoka kati ya makabila yako yote, asimame ili kuhudumu katika jina la Yehova, yeye na wanawe, sikuzote.[a]

6 "Na ikiwa Mlawi ataenda nje ya moja la majiji yako ya Israeli yote, ambapo alikaa kwa muda,[b] naye aje kwa sababu ya tamaa yoyote ya nafsi yake mpaka mahali ambapo Yehova atapachagua,[c] **7** atahudumu pia katika jina la Yehova Mungu wake sawa na ndugu zake wote, Walawi, wanaosimama hapo mbele za Yehova.[d] **8** Atakula fungu linalolingana,[e] mbali na kile anachopata kutokana na vitu anavyouza kati ya mali za mababu zake.

9 "Utakapokuwa umeingia katika nchi ambayo Yehova Mungu wako anakupa wewe, usijifunze kufanya kulinganana na machukizo ya mataifa hayo.[f] **10** Asipatikane ndani yako yeyote anayempitisha mwana wake au binti yake katikati ya moto,[g] yeyote anayefanya uaguzi,[h] mwenye kufanya uchawi[i] au yeyote anayetafuta ishara za bahati[j] au mlozi,[k] **11** au anayefunga wengine kwa kuwatakia maovu[l] au yeyote anayetafuta shauri kwa mwenye kuwasiliana na pepo[m] au mjuzi wa kubashiri matukio[n] au yeyote anayeuliza habari kutoka kwa wafu.[o] **12** Kwa maana kila mtu anayefanya mambo hayo ni chukizo kwa Yehova, na kwa sababu ya machukizo hayo, Yehova Mungu wako anawafukuza kutoka mbele yako.[p] **13** Utajionyesha kuwa huna kosa kwa Yehova Mungu wako.[q]

14 "Kwa maana mataifa haya unayoyafukuza yalikuwa yakiwasikiliza wale wanaofanya uchawi[r] na wale wanaoagua;[s] lakini wewe, Yehova Mu-

SURA 17

a Ayu 31:24
Zb 62:10
1Ti 6:9
b Kum 31:9
Kum 31:26
2Fa 22:8
c 2Nya 34:18
d Kum 11:18
Zb 1:2
Zb 119:97
e 1Sa 15:17
2Nya 32:25
Zb 131:1
Mk 10:42
1Pe 5:5
f Kum 5:32
1Sa 13:13
1Fa 15:5
g Met 10:27

SURA 18

h Hes 18:24
Kum 10:9
Yos 13:33
i Hes 18:8
Yos 13:14
1Ko 9:13
j Hes 18:20
k Kut 23:19
Hes 18:12
Kum 26:10
2Nya 31:4
Ne 12:44

Safu ya 2

a Kut 28:1
Hes 3:10
Kum 10:8
Kum 17:12
b Hes 35:2
c Kum 12:5
Kum 16:2
Zb 26:8
d 2Nya 31:2
e Law 7:10
Lu 10:7
1Ti 5:18
f Law 18:26
Kum 12:30
g Law 18:21
Kum 12:31
2Fa 16:3
2Nya 28:3
Zb 106:37
Yer 19:5
Yer 32:35
h 2Fa 17:17
Mdo 16:16
i Law 19:26
Mdo 19:19
j Eze 21:21
k Kut 22:18
l Isa 47:9
m Law 20:27
1Nya 10:13
n Law 19:31
2Nya 33:6
o 1Sa 28:3
1Sa 28:11
Isa 8:19
Ga 5:20
p Law 18:24
Kum 9:4
q 2Sa 22:24
Zb 37:18
Mt 5:48
2Pe 3:14
r Law 19:26
2Fa 21:2
2Fa 21:6
s Yos 13:22

ngu wako hajakupa kitu chochote kama hicho.[a] **15** Nabii kutoka katikati yako mwenyewe, kutoka kwa ndugu zako, kama mimi, ndiye ambaye Yehova Mungu wako atakuinulia —ninyi mnapaswa kumsikiliza yeye[b]— **16** kulingana na yote uliyomwomba Yehova Mungu wako huko Horebu katika ile siku ya kutaniko,[c] na kusema 'Usiache nisikie tena sauti ya Yehova Mungu wangu, na huu moto mkubwa usiache niuone tena, nisije nikafa.'[d] **17** Ndipo Yehova akaniambia, 'Wamefanya vema katika kusema walilosema.[e] **18** Nitawainulia wao nabii kutoka katikati ya ndugu zao, kama wewe;[f] nami nitaweka maneno yangu katika kinywa chake,[g] naye atasema nao yote nitakayomwamuru.[h] **19** Na itatukia kwamba mtu ambaye hatasikiliza maneno yangu ambayo atayasema katika jina langu, mimi mwenyewe nitamtaka ajibu.[i]

20 "Hata hivyo, nabii atakayethubutu kusema katika jina langu neno ambalo sijamwamuru kusema[j] au atakayesema katika jina la miungu mingine,[k] nabii huyo lazima afe.[l] **21** Na ikiwa utasema moyoni mwako: "Tutajuaje neno ambalo Yehova hajasema?"[m] **22** Nabii anaposema katika jina la Yehova na neno hilo lisitukie au lisitimie, hilo ndilo neno ambalo Yehova hakusema.[n] Kwa kimbelembele nabii huyo alilisema. Usimwogope.'[o]

19 "Yehova Mungu wako atakapokatilia mbali mataifa[p] ambayo nchi yao Yehova Mungu wako anakupa wewe, nawe uwe umewafukuza na kukaa katika majiji yao na nyumba zao,[a] **2** utatenga majiji matatu kwa ajili yako katikati ya nchi yako ambayo Yehova Mungu wako anakupa wewe uimiliki.[b] **3** Utajitayarishia njia, nawe utagawa katika sehemu tatu lile eneo la nchi yako ambayo Yehova Mungu wako alikupa wewe iwe mali yako, nayo itakuwa kwa ajili ya muuaji yeyote, akimbilie humo.[c]

4 "Sasa hii ndiyo hukumu ya muuaji atakayekimbilia humo na ambaye ataishi: Anapompiga na kumuua mwenzake bila kujua naye hakuwa akimchukia hapo kwanza;[d] **5** au anapoenda na mwenzake msituni kukusanya kuni, na mkono wake umeinuliwa ili kugonga kwa shoka ili kuukata mti, nacho chuma kiwe kimechomoka kutoka katika mpini wa mbao,[e] na kiwe kimemgonga mwenzake naye akafa, yeye mwenyewe atakimbilia moja la majiji hayo naye ataishi.[f] **6** Kama sivyo mlipiza-kisasi[g] cha damu, kwa sababu moyo wake una moto, anaweza kumfuatilia muuaji, amfikie, kwa kuwa njia ni ndefu; naye anaweza kuipiga nafsi yake na kuiua, ingawa hakuna hukumu ya kifo[h] kwa ajili yake, kwa sababu hakuwa akimchukia hapo kwanza. **7** Ndiyo sababu ninakuamuru wewe, na kusema, 'Utajitengea majiji matatu.'[i]

8 "Na ikiwa Yehova Mungu wako atalipanua eneo lako kulingana na jambo alilowaapia mababu zako,[j] naye amekupa wewe nchi yote aliyoahidi kuwapa mababu zako,[k] **9** kwa sababu utaishika amri yote hii ninayokuamuru wewe leo kwa kuifanya, kumpenda Yehova Mungu wako na kutembea

SURA 18
a Zb 147:20; Mdo 14:16
b Mwa 49:10; Hes 24:17; Lu 7:16; Lu 24:19; Yoh 1:45; Yoh 6:14; Mdo 3:22; Mdo 7:37
c Kut 19:17; Kum 9:10
d Kut 20:19
e Kum 5:28
f Kut 34:28; Hes 12:3; Mal 3:1; Mt 4:2; Mt 11:29; Lu 24:27; Lu 24:44; Yoh 5:46
g Yoh 8:28; Yoh 17:8
h Yoh 12:49; Yoh 15:15; Ebr 1:2
i Mdo 3:23
j Kum 13:1; Yer 14:14; Yer 28:11; Eze 13:6; Mt 7:15
k Kum 13:2; 1Fa 18:19; Yer 23:13
l Kum 13:5; Yer 27:15; Zek 13:3
m 1Yo 4:1
n Yer 28:15
o Met 29:25

SURA 19
p Kut 34:24; Yos 24:8

Safu ya 2
a Kum 6:10; Kum 7:1; Kum 9:1; Kum 12:29
b Kut 21:13; Hes 35:14; Yos 20:7
c Yos 20:9
d Hes 35:15; Kum 4:42
e 2Fa 6:5
f Hes 35:25
g Hes 35:12; Hes 35:19; Yos 20:5; 2Sa 14:7
h Kum 17:8; Yos 20:4; 2Nya 19:10
i Kum 19:2
j Mwa 15:18; Kut 23:31; Kum 11:24
k Mwa 28:14; Kum 12:20

katika njia zake sikuzote,[a] basi utajiongezea majiji mengine matatu kwa majiji haya matatu,[b] **10** ili damu isiyo na hatia[c] isimwagwe katikati ya nchi yako ambayo Yehova Mungu wako anakupa wewe iwe urithi, na hatia yoyote ya damu isiwe juu yako.[d]

11 "Lakini ikiwa kutakuwako mtu anayemchukia[e] mwenzake, naye amemvizia, akainuka juu yake, akaipiga nafsi yake na kuiua naye amekufa,[f] na mtu huyo amekimbilia moja la majiji hayo, **12** ndipo wanaume wazee wa jiji lake watatuma watu na kumchukua kutoka humo, nao watamtia mkononi mwa mlipiza-kisasi cha damu, naye lazima afe.[g] **13** Jicho lako lisimsikitikie,[h] nawe lazima uondolee mbali hatia ya damu isiyo na hatia kutoka katika Israeli,[i] ili uwe na mema.

14 "Usisogeze nyuma alama za mpaka wa mwenzako,[j] wakati ambapo mababu watakuwa wameweka mipaka katika urithi wako ambao utarithi katika nchi ambayo Yehova Mungu wako anakupa wewe uimiliki.

15 "Shahidi mmoja asiinuke juu ya mtu kuhusu kosa au dhambi yoyote,[k] kuhusu dhambi yoyote ambayo huenda akafanya. Kwa kinywa cha mashahidi wawili au kwa kinywa cha mashahidi watatu jambo hilo litathibitishwa vizuri.[l] **16** Ikiwa shahidi anayepanga hila ya jeuri atainuka juu ya mtu na kuleta shtaka la maasi juu yake,[m] **17** ndipo watu hao wawili wenye mzozo watakaposimama mbele za Yehova, mbele ya makuhani na waamuzi watakaokuwa wakitenda siku hizo.[a] **18** Na waamuzi watatafuta kabisa,[b] na ikiwa shahidi huyo ni shahidi wa uwongo naye ameleta shtaka la uwongo juu ya ndugu yake, **19** ndipo mtakapomfanyia kama vile alivyompangia ndugu yake hila,[c] nawe utaondolea mbali kilicho kibaya kutoka katikati yako.[d] **20** Kwa hiyo wale wanaobaki watasikia na kuogopa, nao hawatafanya tena kamwe jambo baya kama hilo katikati yako.[e] **21** Na jicho lako lisisikitike:[f] nafsi itakuwa kwa nafsi, jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu.[g]

20 "Ikiwa utaenda katika pigano juu ya adui zako nawe uone farasi na magari ya vita,[h] watu wengi kuliko wewe, usiwaogope; kwa maana Yehova Mungu wako yuko pamoja nawe,[i] aliyekutoa katika nchi ya Misri.[j] **2** Na itatukia kwamba mtakapokuwa mmekaribia pigano, ndipo kuhani atakapokaribia na kusema na watu.[k] **3** Naye atawaambia, 'Sikieni, Ee Israeli, mnakaribia leo kupigana na adui zenu. Msiache mioyo yenu iogope.[l] Msiogope na kukimbia kwa wasiwasi au kutetemeka kwa sababu yao,[m] **4** kwa maana Yehova Mungu wenu anapiga mwendo pamoja nanyi ili kupigana kwa ajili yenu juu ya adui zenu apate kuwaokoa ninyi.'[n]

5 "Maofisa[o] pia watasema na watu, na kuwaambia, 'Ni nani ambaye amejenga nyumba mpya naye hajaizindua? Na aende na kurudi nyumbani kwake, asije akafa vitani

SURA 19
a Kum 11:22; Kum 12:32; 1Yo 5:3
b Yos 20:8
c Kum 21:9; 2Fa 21:16; Met 6:17; Yer 7:6; Yon 1:14; Mt 27:4
d Zb 5:6; Zb 55:23; Mdo 20:26
e Mt 15:19; 1Yo 3:15
f Kut 21:12; Hes 35:16; Kum 27:24
g Mwa 9:6; 1Fa 2:5; 1Fa 2:31
h Kum 19:21
i Law 24:17; Law 24:21; Hes 35:33; Kum 21:9; 2Sa 21:1
j Kum 27:17; Ayu 24:2; Met 23:10
k Hes 35:30; Kum 17:6
l 1Fa 21:10; Mt 18:16; Mt 26:60; Yoh 8:17; 2Ko 13:1; 1Ti 5:19; Ebr 10:28
m Kut 23:1; 1Fa 21:13; Zb 27:12; Mk 14:56

Safu ya 2
a Kum 17:9; Kum 21:5
b Kum 13:14; Kum 17:4; 2Nya 19:6; Ayu 29:16
c Met 19:5; Da 6:24
d Kum 21:21; Kum 24:7; 1Ko 5:13
e Kum 13:11; Kum 17:13; 1Ti 5:20
f Kum 19:13
g Kut 21:23; Law 24:20; Mt 5:38

SURA 20
h Yos 11:4
i Kum 3:22; Kum 31:6; Zb 20:7; Zb 46:7; Met 21:31; Ro 8:31
j Kut 13:3
k Hes 31:6; Amu 20:28; 1Sa 30:7; 2Nya 13:12
l Zb 27:3; Isa 35:4; Isa 41:10
m Zb 3:6
n Kut 14:14; Kum 32:30; Yos 23:10

o Hes 31:14; Kum 16:18.

na mwanamume mwingine aizindue.[a] **6** Na ni nani ambaye amepanda shamba la mizabibu naye hajaanza kutumia matunda yake? Na aende na kurudi nyumbani kwake, asije akafa vitani na mwanamume mwingine akaanza kutumia matunda yake.[b] **7** Na ni nani ambaye amemchumbia mwanamke naye hajamchukua? Na aende na kurudi nyumbani kwake,[c] asije akafa vitani na mwanamume mwingine amchukue mwanamke huyo.' **8** Nao maofisa watazidi kusema na watu na kuwaambia, 'Ni nani mwoga na mwenye moyo dhaifu?[d] Na aende na kurudi nyumbani kwake, asije akasababisha mioyo ya ndugu zake iyeyuke kama moyo wake mwenyewe.'[e] **9** Na itatukia kwamba wakati ambapo maofisa hao watakuwa wamemaliza kusema na watu, ndipo watakapoweka pia wakuu wa majeshi mbele ya watu.

10 "Ikiwa utakaribia jiji ili kupigana nalo, utalitangazia pia masharti ya amani.[f] **11** Na itatukia kwamba ikiwa litakutolea jibu la amani nalo limekufungulia, itatukia pia kwamba watu wote watakaopatikana ndani yake watakuwa wako kwa ajili ya kazi ya kulazimishwa, nao watakutumikia.[g] **12** Lakini lisipofanya amani pamoja nawe,[h] nalo lifanye vita pamoja nawe, nawe ulazimike kulizingira, **13** Yehova Mungu wako hakika atalitia mkononi mwako, nawe utampiga kila mwanamume aliye ndani yake kwa makali ya upanga.[i] **14** Utapora kwa ajili yako[j] wanawake tu na watoto wadogo[k] na wanyama wa kufugwa[l] na kila kitu kitakachokuwa jijini, nyara zake zote; nawe utakula nyara za adui zako, ambao Yehova Mungu wako amekupa wewe.[a]

15 "Hivyo ndivyo utakavyoyafanyia majiji yote yaliyo mbali sana nawe ambayo si majiji ya mataifa haya. **16** Ni katika majiji ya watu hawa tu ambayo Yehova anakupa yawe urithi ambayo hutaacha hai chochote kinachopumua,[b] **17** kwa sababu lazima utawaangamiza, Wahiti na Waamori, Wakanaani na Waperizi, Wahivi na Wayebusi,[c] kama vile ambavyo Yehova Mungu wako amekuamuru; **18** ili wasiwafundishe kulingana na machukizo yao yote, ambayo wameifanyia miungu yao, nanyi mumtendee dhambi Yehova Mungu wenu.[d]

19 "Ikiwa utazingira jiji siku nyingi kwa kupigana nalo ili kuliteka, usiharibu miti yake kwa kutumia shoka juu yake; kwa maana utakula kutokana nayo, nawe usiikate na kuiangusha,[e] kwani mti wa shamba je, ni mtu ndipo uuzingire? **20** Ila mti ambao wewe unajua kwamba si mti wa chakula, huo ndio unaopaswa kuharibu, nawe utaukata na kujenga mazingiwa[f] juu ya jiji linalofanya vita nawe, mpaka lianguke.

21 "Ikiwa mtu atapatikana akiwa ameuawa katika nchi ambayo Yehova Mungu wako anakupa uimiliki, akiwa ameanguka uwanjani, na haijajulikana ni nani aliyempiga na kumuua,[g] **2** wanaume wako wazee na waamuzi[h] wako watatoka nje na kupima mpaka kwenye majiji yanayomzunguka mtu aliyeuawa; **3** na itakuwa ni lile jiji lililo karibu zaidi na yule aliyeuawa. Nao

SURA 20
a Mhu 2:24
b Zb 145:9; Mhu 3:13
c Kum 24:5
d Amu 7:3
e Hes 13:33; Hes 14:1; Hes 32:9; Kum 1:28; Mdo 21:13
f Yos 11:19
g Law 25:46; Kum 20:15; Yos 9:22; Yos 9:27
h Zb 120:7
i Hes 31:7
j Hes 31:12; Hes 31:27; 2Nya 14:13; Zb 68:12
k Hes 31:9; Hes 31:18
l Yos 8:2

Safu ya 2
a Yos 22:8
b Yos 6:17; Yos 10:28; Yos 11:11
c Kum 7:1
d Kut 34:15; Kum 7:4; Yos 23:12; Zb 106:35; Isa 2:6; 1Ko 5:6; 1Ko 15:33
e Ne 9:25
f 2Nya 26:15; Mhu 9:14; Isa 37:33; Yer 6:6; Eze 17:17

SURA 21
g Zb 9:12; Met 28:17; Isa 26:21
h Kum 16:18

wanaume wazee wa jiji hilo wa-
tamchukua ng'ombe mchanga
kutoka kati ya mifugo ambaye
hajafanya kazi, ambaye hajavu-
ta nira; **4** na wanaume wazee
wa jiji hilo watampeleka ng'o-
mbe huyo mpaka kwenye bo-
nde la mto wenye maji yanayo-
tiririka ambapo kidesturi hapa-
kuwa na kulima wala kupanda
mbegu, nao watavunja shingo
ya ng'ombe huyo mchanga ka-
tika bonde hilo la mto.[a]

5 "Na makuhani wana wa
Lawi watakaribia, kwa sa-
babu hao ndio Yehova Mungu
wako amechagua wamhudu-
mie[b] na kulisifu[c] jina la Yeho-
va na ambao kwa kinywa chao
kila mzozo juu ya kila tendo
lenye jeuri, wapasa kuondole-
wa mbali.[d] **6** Kisha wanaume
wote wazee wa jiji hilo walio
karibu zaidi na mtu aliyeuawa
wataosha mikono yao[e] juu ya
yule ng'ombe mchanga, amba-
ye shingo yake ilivunjwa kati-
ka lile bonde la mto; **7** nao
watajibu na kusema, 'Mikono
yetu haikumwaga damu hii,
wala macho yetu hayakuona
ikimwagwa.[f] **8** Usiihesabie
watu wako Israeli, ambao uli-
komboa,[g] Ee Yehova, wala usi-
weke katikati ya watu wako
Israeli hatia ya damu isiyo na
hatia.'[h] Na wasihesabiwe ha-
tia hiyo ya damu. **9** Na wewe
—wewe utaondolea mbali hatia
ya damu kutoka katikati yako,[i]
kwa sababu utafanya yaliyo
sawa machoni pa Yehova.[j]

10 "Ikiwa utaenda vitani ku-
pigana na adui zako na Yeho-
va Mungu wako awe amewatia
mkononi mwako[k] nawe uwa-
chukue mateka;[l] **11** nawe
uone kati ya mateka hao
mwanamke mwenye umbo zuri,

SURA 21

a Hes 35:33
b Kut 28:1
Kum 18:5
c Hes 6:23
1Nya 23:13
d Kum 17:9
Kum 19:17
Mal 2:7
e Zb 26:6
Mt 27:24
f 2Sa 3:28
Zb 7:3
g Kum 13:5
2Sa 7:23
h Hes 16:22
Yer 26:15
Yon 1:14
i Kum 19:13
j Kum 13:18
Zb 11:4
Met 15:3
Ebr 4:13
k Kum 20:13
Yos 21:44
l Hes 31:9
Kum 20:14

Safu ya 2

a Mwa 29:20
Mwa 34:3
Amu 14:2
b Isa 3:24
1Ko 11:6
c Hes 20:29
Kum 34:8
d Kum 24:1
e Law 25:46
f Mwa 29:30
Mwa 29:33
1Sa 1:4
g 2Nya 21:3
h 1Nya 5:1
i Mwa 49:3
Zb 105:36
j Mwa 25:31
Ebr 12:16

nawe ushikamane naye[a] na ku-
mchukua awe mke wako,
12 ndipo utakapomleta ndani
ya nyumba yako. Lazima anyoe
kichwa chake,[b] atunze ku-
cha zake, **13** na kuvua nguo
ya kujitanda ya utekwa wake,
akae katika nyumba yako, amli-
lie baba yake na mama yake
kwa mwezi mzima;[c] na baada
ya jambo hilo utalala naye,
nawe utamchukua awe bibi-
arusi wako, naye atakuwa mke
wako. **14** Na itatukia kwa-
mba ikiwa hukupendezwa
naye, basi utamwacha aende
zake,[d] kama inavyopenda nafsi
yake mwenyewe; lakini huta-
muuza kamwe kwa ajili ya
pesa. Usimwonee[e] baada ya ku-
mfedhehesha.

15 "Ikiwa mwanamume ata-
kuwa na wake wawili, mmo-
ja anayependwa na mwingine
anayechukiwa, nao, yule ana-
yependwa na yule anayechu-
kiwa, wamzalie wana, na iwe
kwamba mwana mzaliwa wa
kwanza ni wa yule anayechuki-
wa,[f] **16** pia itatukia kwamba
katika siku ambayo atawapa
wanawe urithi wa vitu alivyo
navyo, hataruhusiwa kumfa-
nya mwana wa yule anayepe-
ndwa awe mzaliwa wake wa
kwanza kwa hasara ya mwana
wa yule anayechukiwa, mzali-
wa wa kwanza.[g] **17** Kwa ma-
ana anapaswa kumtambua
mwana wa yule anayechuki-
wa kuwa mzaliwa wa kwanza
kwa kumpa sehemu mbili za
kila kitu alicho nacho,[h] kwa
sababu huyo ndiye mwanzo
wa nguvu zake za uzazi.[i] Haki
ya cheo cha mzaliwa wa kwa-
nza ni yake.[j]

18 "Ikiwa mtu atakuwa na
mwana ambaye ni mkaidi na

mwasi,[a] awe hasikilizi sauti ya baba yake au sauti ya mama yake,[b] nao wamemrekebisha bali yeye hawasikilizi,[c]
19 baba yake na mama yake watamshika na kumtoa nje mpaka kwa wanaume wazee wa jiji lake na kwenye lango la mahali pake,[d] **20** nao watawaambia wanaume wazee wa jiji lake, 'Huyu mwana wetu ni mkaidi na mwasi; hasikilizi sauti yetu,[e] ni mlafi[f] na mlevi.'[g]
21 Ndipo watu wote wa jiji watampiga kwa mawe, naye lazima afe. Kwa hiyo mtaondolea mbali kilicho kibaya kutoka kati yenu, na Israeli wote watasikia na kuogopa kwelikweli.[h]

22 "Na ikiwa mtu atakuwa na dhambi inayostahili hukumu ya kifo, naye ameuawa,[i] nawe umemtundika juu ya mti,[j]
23 maiti yake isibaki usiku kucha juu ya mti;[k] bali kwa vyovyote utamzika siku hiyo, kwa sababu mtu aliyetundikwa ni kitu kilicholaaniwa na Mungu;[l] nawe usiitie unajisi nchi yako, ambayo Yehova Mungu wako anakupa iwe urithi.[m]

22 "Usimwone ng'ombe wa ndugu yako au kondoo wake akipotea njia nawe uwaache kimakusudi.[n] Kwa vyovyote unapaswa kuwarudisha kwa ndugu yako.[o] **2** Na ikiwa ndugu yako hayuko karibu nawe na wewe hujamjua, utamleta mnyama huyo nyumbani mwako, naye atakaa nawe mpaka ndugu yako awe amemtafuta. Nawe utamrudisha kwake.[p] **3** Hivyo ndivyo pia utakavyofanya na punda wake, na hivyo ndivyo utakavyofanya na nguo yake ya kujitanda, na hivyo ndivyo utakavyofanya na kitu chochote kilichopotea cha ndugu yako, kinachopotea kutoka kwake na ambacho umepata. Hutaruhusiwa kukiacha.

4 "Usimwone punda wa ndugu yako au ng'ombe wake akianguka barabarani nawe uwaache kimakusudi. Kwa vyovyote unapaswa kuwasaidia na kuwainua.[a]

5 "Vazi lolote la mwanamume lisivaliwe na mwanamke, wala mwanamume asivae nguo ya kujitanda ya mwanamke;[b] kwa maana mtu yeyote anayefanya mambo hayo ni chukizo kwa Yehova Mungu wako.

6 "Ikiwa kiota cha ndege kitakuwa mbele yako njiani, katika mti wowote au chini kikiwa na vifaranga[c] au mayai, naye mama anakalia vifaranga au mayai, usimchukue mama pamoja na watoto.[d]
7 Kwa vyovyote unapaswa kumwacha mama aende zake, lakini unaweza kuchukua watoto; ili mambo yapate kukuendea vema wewe, nawe urefushe siku zako.[e]

8 "Ikiwa utajenga nyumba mpya, pia utafanya ukuta wa ukingoni kwa ajili ya dari lako,[f] ili usiletee nyumba yako hatia ya damu kwa sababu mtu anaweza kuanguka kutoka hapo.

9 "Usipande shamba lako la mizabibu aina mbili za mbegu,[g] mazao kamili ya mbegu hiyo ambayo huenda ukapanda na mazao ya shamba la mizabibu yasije yakatwaliwa na patakatifu.

10 "Usilime kwa ng'ombedume na punda pamoja.[h]

11 "Usivae kitu kilichochanganywa cha sufu na kitani pamoja.[i]

SURA 21
a Met 30:11
b Kut 20:12
Kum 27:16
Met 1:8
Met 20:20
Eze 22:7
Efe 6:1
c Kum 8:5
Met 13:24
Met 19:18
Met 23:13
Ebr 12:9
d Kum 16:18
e Met 15:5
Met 19:26
Met 30:17
f Met 23:20
Met 28:7
g Met 20:1
Met 23:21
Ro 13:13
1Ko 6:10
Efe 5:18
h Kum 13:11
i Hes 25:5
2Sa 4:12
j Yos 10:26
Mdo 10:39
k Yos 8:29
Yoh 19:31
l 2Ko 5:21
Ga 3:13
m Hes 35:34

SURA 22
n Kut 23:4
o Zek 7:9
p Met 24:12
Mt 7:12

Safu ya 2
a Kut 23:5
Law 19:18
Lu 10:27
Ga 6:10
b 1Ti 2:9
c Lu 12:6
d Law 22:28
Zb 36:6
Zb 145:9
Met 12:10
Mt 10:29
e Kum 4:40
Met 3:2
f 2Sa 11:2
Mdo 10:9
g Law 19:19
h Met 12:10
i Law 19:19

12 "Utajifanyia shada kwenye miisho minne ya mavazi
yako ambayo wewe hujifunika
nayo.[a]
13 "Ikiwa mwanamume ata-
mchukua mwanamke, alale
naye, na aje kumchukia,[b]
14 naye awe amemshtaki mwa-
namke huyo kuwa mwenye
matendo yenye sifa mbaya na
kuleta jina baya[c] juu yake, naye
amesema, 'Mwanamke huyu
nimemchukua, nikamkari-
bia, nami sikupata uthibiti-
sho wa ubikira ndani yake';[d]
15 baba ya msichana huyo na
mama yake wataleta uthibi-
tisho wa ubikira wa msicha-
na huyo kwa wanaume wazee
wa jiji hilo kwenye lango lake;[e]
16 naye baba ya msichana ata-
waambia wanaume wazee, 'Ni-
limpa mwanamume huyu bi-
nti yangu awe mke wake, naye
akamchukia.[f] **17** Na tazama,
anamshtaki juu ya matendo ye-
nye sifa mbaya,[g] na kusema:
"Nimepata kujua kwamba binti
yako hana uthibitisho wa ubiki-
ra."[h] Sasa huu ndio uthibitisho
wa ubikira wa binti yangu.' Nao
watatandaza nguo hiyo ya ku-
jitanda mbele ya wanaume wa-
zee wa jiji hilo. **18** Nao wa-
naume wazee[i] wa jiji hilo wa-
tamchukua mwanamume huyo
na kumtia nidhamu.[j] **19** Nao
watamtoza shekeli mia moja na
kumpa baba ya msichana huyo,
kwa sababu alileta jina baya juu
ya bikira wa Israeli;[k] naye ataen-
delea kuwa mke wake. Hata-
ruhusiwa kumtaliki siku zake
zote.
20 "Hata hivyo, ikiwa jambo
hilo limeonekana kuwa kweli,
uthibitisho wa ubikira haukupa-
tikana ndani ya msichana huyo,[l]
21 watamtoa nje msichana huyo
kwenye mlango wa nyumba ya
baba yake, nao watu wa jiji lake
watampiga kwa mawe, naye la-
zima afe, kwa sababu amefa-
nya upumbavu wenye kufedhe-
hesha[a] katika Israeli kwa kufa-
nya ukahaba katika nyumba ya
baba yake.[b] Kwa hiyo lazima uta-
ondolea mbali lililo baya kuto-
ka katikati yako.[c]
22 "Ikiwa mwanamume ata-
patikana akilala na mwanamke
aliye na mume,[d] wote wawi-
li watauawa pamoja, yule mwa-
k Kum 8:19; Yos 23:15
l Kum 4:26; Kum 31:28; Isa 1:2
m Kum 32:47
n Kum 11:26; Kum 28:2
o Kum 27:26; Kum 28:15
p Yos 24:15
q Kum 6:2; Yer 32:39
r Kum 10:12
s Kum 4:4
t Kum 4:40
u Mwa 12:7; Mwa 15:18

SURA 31

v Kut 7:7; Kum 34:7; Mdo 7:23

ndani,[a] kama vile Yehova alivyoniambia, ‘Wewe hutavuka mto huu wa Yordani.’[b] **3** Yehova Mungu wako ndiye anayevuka mbele yako.[c] Yeye mwenyewe atayaangamiza mataifa haya kutoka mbele yako, na wewe lazima uyafukuzie mbali.[d] Yoshua ndiye anayevuka mbele yako,[e] kama alivyosema Yehova. **4** Na hakika Yehova atawatendea wao kama alivyowatendea Sihoni[f] na Ogu,[g] wafalme wa Waamori, na nchi yao, alipowaangamiza hao.[h] **5** Na Yehova amewatia mkononi mwenu,[i] nanyi lazima mwatendee kulingana na amri yote ambayo nimewaamuru ninyi.[j] **6** Iweni hodari na wenye nguvu.[k] Usiogope wala kushtuka mbele yao,[l] kwa sababu Yehova Mungu wako ndiye anayepiga mwendo pamoja nawe. Hatakutupa wala kukuacha kabisa.”[m]

7 Na Musa akamwita Yoshua na kumwambia mbele ya macho ya Israeli wote: “Uwe hodari na mwenye nguvu,[n] kwa sababu wewe—wewe utawaingiza watu hawa katika nchi ambayo Yehova aliwaapia mababu zao kwamba atawapa, na wewe mwenyewe utawapa iwe urithi.[o] **8** Na Yehova ndiye anayepiga mwendo mbele yako. Yeye mwenyewe ataendelea kuwa pamoja nawe.[p] Hatakutupa wala kukuacha kabisa. Usiogope wala usiingiwe na hofu.”[q]

9 Ndipo Musa akaandika sheria hii[r] na kuwapa makuhani wana wa Lawi,[s] wachukuaji wa sanduku la agano la Yehova,[t] na kuwapa wanaume wote wazee wa Israeli. **10** Na Musa akawaamuru, na kusema: “Mwishoni mwa kila miaka saba, katika wakati uliowekwa wa mwaka wa kuachilia huru,[a] katika sherehe ya vibanda,[b] **11** wakati ambapo Israeli wote watakuja kuuona uso wa Yehova[c] Mungu wako katika mahali atakapopachagua,[d] utaisoma sheria hii mbele ya Israeli wote masikioni mwao.[e] **12** Wakutanishe watu,[f] wanaume na wanawake na watoto wadogo na mkaaji mgeni aliye ndani ya malango yako, ili wasikilize na ili wajifunze,[g] kwa maana ni lazima wamwogope Yehova Mungu[h] wenu na kuwa waangalifu kuyatimiza maneno yote ya sheria hii. **13** Na wana wao ambao hawakujua wanapaswa kusikiliza,[i] nao lazima wajifunze kumwogopa Yehova Mungu wenu siku zote ambazo ninyi mnakaa juu ya nchi ambayo mnavuka Yordani ili kuimiliki.”[j]

14 Baada ya jambo hilo Yehova akamwambia Musa: “Tazama! Siku za kufa kwako zimekaribia.[k] Mwite Yoshua, na usimame katika hema la mkutano, ili nimpe utume.”[l] Basi Musa na Yoshua wakaenda na kusimama katika hema la mkutano.[m] **15** Ndipo Yehova akaonekana katika hema katika nguzo ya wingu, na hiyo nguzo ya wingu ikaanza kusimama kwenye mlango wa hema.[n]

16 Sasa Yehova akamwambia Musa: “Tazama! Unalala pamoja na mababu zako;[o] na hakika watu hawa watainuka[p] na kufanya uasherati na miungu migeni ya nchi wanayoiendea,[q] kati yao, nao hakika wataniacha[r] na kuvunja agano langu ambalo nimefanya pamoja nao.[s] **17** Ndipo hasira

SURA 31

a Hes 27:17
b Hes 20:12
Kum 3:27
Kum 4:21
c Kum 9:3
d Zb 44:2
e Hes 27:18
Kum 3:28
Yos 1:2
Yos 4:14
Mdo 7:45
f Hes 21:24
g Hes 21:35
h Kut 23:23
Kum 29:7
i Kum 3:21
Kum 7:2
j Hes 33:52
Kum 7:24
Kum 20:16
k Yos 1:6
Zb 27:14
Zb 118:6
l Hes 14:9
Kum 1:29
Kum 7:18
Zb 56:3
m Kum 4:31
Yos 1:5
Ebr 13:5
n Yos 10:25
Efe 6:10
o Kum 1:38
p Kut 33:14
q Yos 1:9
r Kut 34:27
Da 9:13
s Kum 17:18
t Hes 4:15
Kum 31:25

Safu ya 2

a Kum 15:1
b Law 23:34
c Kut 23:17
Kum 16:16
d Kum 12:5
e Ne 8:7
f Kum 4:10
Ebr 10:25
g Kum 29:29
h Zb 34:11
Met 8:13
i Kum 6:7
Kum 11:2
Zb 78:6
Met 22:6
Efe 6:4
j Kum 30:16
k Hes 27:13
Kum 31:2
l Kum 3:28
m Kut 40:2
n Kut 33:9
Kut 40:38
Zb 99:7
o 2Sa 7:12
Yoh 3:13
p Kut 32:6
q Kut 34:15
Amu 2:17
Zb 106:37
Zb 106:39
Yer 3:1
Eze 16:15
r Kum 32:15
Amu 2:12
1Fa 11:33
s Amu 2:20
Yer 31:32
Ebr 8:9

yangu itakapowaka kwelikweli
juu yao katika siku hiyo,[a] nami
hakika nitawaacha[b] na kuufi-
cha uso wangu mbali nao,[c] nao
watakuwa kitu cha kuteketez-
wa; na misiba mingi na taabu
zitakuja juu yao,[d] nao watalazi-
mika kusema siku hiyo, 'Je, mi-
siba hii haikuja juu yetu kwa
sababu Mungu wetu hayuko ka-
tikati yetu?'[e] **18** Mimi nami,
nitauficha kabisa uso wangu ka-
tika siku hiyo kwa sababu ya
ubaya wote ambao wameute-
nda, kwa sababu wameigeukia
miungu mingine.[f]
19 "Na sasa jiandikieni we-
nyewe wimbo huu[g] na kuwafu-
ndisha wana wa Israeli.[h] Uwe-
keni katika vinywa vyao ili wi-
mbo huu upate kuwa shahidi
wangu juu ya wana wa Isra-
eli.[i] **20** Kwa maana nitawale-
ta katika nchi ambayo nimewa-
apia mababu zao,[j] inayotiririka
maziwa na asali,[k] nao haki-
ka watakula[l] na kushiba na
kunenepa[m] na kuigeukia mi-
ungu mingine,[n] nao kwa
kweli wataitumikia na kunite-
ndea bila heshima na kulivunja
agano langu.[o] **21** Na itatukia
kwamba wakati ambapo misiba
mingi na taabu zitawajia,[p] wi-
mbo huu lazima pia utashuhu-
dia mbele yao, kwa sababu ha-
upaswi kusahauliwa katika vi-
nywa vya uzao wao, kwa maa-
na najua vema mwelekeo wao[q]
wanaousitawisha leo kabla sija-
waingiza katika nchi niliyowaa-
pia."
22 Kwa hiyo Musa akaandi-
ka wimbo huu katika siku hiyo,
ili awafundishe wana wa Isra-
eli.[r]
23 Naye akampa utume Yo-
shua mwana wa Nuni[s] na ku-
sema: "Uwe hodari na mwe-
nye nguvu,[a] kwa sababu wewe
—wewe utawaingiza wana wa
Israeli katika nchi ambayo ni-
mewaapia,[b] na mimi mwenye-
we nitaendelea kuwa pamoja
nawe."
24 Na ikawa kwamba mara
tu Musa alipomaliza kuandi-
ka maneno ya sheria hii ka-
tika kitabu mpaka yakaisha,[c]
25 Musa akaanza kuwaamu-
ru Walawi, wachukuaji wa sa-
nduku la agano la Yehova,[d]
na kusema: **26** "Mkichukue
kitabu hiki cha sheria,[e] na-
nyi mkiweke kando ya sandu-
ku[f] la agano la Yehova Mu-
ngu wenu, nacho kitashuhudia
hapo juu yenu.[g] **27** Kwa maa-
na mimi—mimi najua vema
uasi[h] wenu na shingo yenu ngu-
mu.[i] Ikiwa wakati ambapo ni-
ngali hai pamoja nanyi leo,
mmekuwa wenye tabia ya ku-
mwasi Yehova,[j] itakuwaje basi
baada ya kifo changu! **28** Ni-
kutanishie wanaume wote wa-
zee wa makabila yenu na ma-
ofisa wenu,[k] na acheni nise-
me masikioni mwao maneno
haya, na acheni nichukue mbi-
ngu na dunia ziwe mashahidi
dhidi yao.[l] **29** Kwa maana na-
jua vema kwamba baada ya
kifo changu hakika mtatenda
kwa uharibifu,[m] nanyi haki-
ka mtageuka kando kutoka ka-
tika njia ambayo nimewaamu-
ru ninyi; na msiba[n] lazima uta-
waangukia mwishoni mwa siku
hizo, kwa sababu mtafanya ya-
liyo mabaya machoni pa Yehova
ili kumtia uchungu kwa kazi za
mikono yenu."[o]
30 Naye Musa akasema ma-
sikioni mwa kutaniko lote la
Israeli maneno ya wimbo huu
mpaka yakaisha:[p]

SURA 31

a Kum 29:20
Zb 74:1
b 1Nya 28:9
2Nya 15:2
2Nya 24:20
c Kum 32:20
Ayu 34:29
Zb 27:9
Zb 104:29
Eze 39:23
d Kum 31:21
Kum 32:23
Ne 9:27
Met 1:27
e Amu 6:13
f Isa 8:17
Isa 59:2
g Kum 31:30
Kum 32:44
Kol 3:16
h Kum 4:9
Kum 11:19
i Kum 31:21
j Mwa 15:18
Kum 6:10
k Kut 3:8
Hes 13:27
Eze 20:6
l Kum 8:12
Ne 9:25
m Kum 32:15
n Kum 32:16
o Kut 24:7
Kum 29:1
Ne 9:26
p Kum 28:59
Kum 29:22
q Mwa 8:21
Kut 16:4
1Nya 28:9
Zb 139:2
r Kum 31:19
s Hes 27:18
Kum 31:14

Safu ya 2

a Yos 1:6
Zb 27:14
Zb 118:6
b Kum 1:38
Kum 3:28
c Kut 34:27
Kum 31:9
d Hes 4:15
1Nya 15:12
e Kum 17:18
Kum 31:9
2Fa 22:8
2Nya 34:14
f 1Fa 8:9
Ebr 9:4
g Kum 31:19
h Kum 9:24
Kum 32:20
Yos 1:18
Ne 9:26
i Kut 32:9
Kum 9:6
Zb 75:5
Met 29:1
Isa 48:4
j Kum 9:24
Zb 78:8
k Kum 29:10
l Kum 4:26
Kum 30:19
Kum 32:1
m Kum 32:5
Amu 2:19
Ho 9:9
n Kum 28:15
o Yer 44:8
p Kum 32:44

32 "Tegeni sikio, enyi mbingu, nami niseme;
Dunia na isikie maneno ya kinywa changu.[a]
2 Mafundisho yangu yatatiririka kama mvua,[b]
Maneno yangu yatadondoka kama umande,[c]
Kama mvua ya rasharasha juu ya majani[d]
Na kama manyunyu mengi juu ya mimea[e]
3 Kwa maana mimi nitatangaza jina la Yehova.[f]
Nanyi mhesabieni ukuu Mungu wetu![g]
4 Yeye Mwamba, kazi zake ni kamilifu,[h]
Kwa maana njia zake zote ni haki.[i]
Mungu wa uaminifu,[j] ambaye hana ukosefu wowote wa haki;[k]
Yeye ni mwadilifu na mnyoofu.[l]
5 Wametenda kwa uharibifu;[m]
Wao si watoto wake, kasoro ni yao wenyewe.[n]
Kizazi kilicho kombo na kilichopotoka![o]
6 Je, Yehova ndiye mnayeendelea kumfanyia hivi,[p]
Enyi watu wajinga na ambao hawana hekima?[q]
Je, yeye si Baba yenu aliyewazaa,[r]
Yeye aliyewafanyiza ninyi na kuwaimarisha?[s]
7 Kumbuka siku za kale,[t]
Fikirieni miaka iliyopita kutoka kizazi mpaka kizazi;
Muulize baba yako, naye anaweza kukuambia;[u]
Wanaume wenu wazee, nao wanaweza kukuambia.[a]
8 Wakati Aliye Juu Zaidi alipoyapa mataifa urithi,[b]
Alipowatenganisha wana wa Adamu,[c]
Ndipo alipoweka mpaka wa vikundi vya watu[d]
Kuhusiana na hesabu ya wana wa Israeli.[e]
9 Kwa maana fungu la Yehova ni watu wake;[f]
Yakobo ndiye mgawo anaorithi.[g]
10 Alimpata katika nchi ya nyika,[h]
Na katika jangwa tupu, lenye kulia.[i]
Alianza kumzunguka,[j] kumtunza,[k]
Kumlinda kama mboni ya jicho lake.[l]
11 Kama vile tai anavyokitikisa kiota chake,
Anavyoelea angani juu ya watoto wake,[m]
Anavyotandaza mabawa yake, na kuwachukua,
Anavyowachukua kwenye manyoya yake,[n]
12 Ndivyo Yehova peke yake alivyoendelea kumwongoza,[o]
Na hapakuwa na mungu yeyote wa kigeni pamoja naye.[p]
13 Aliendelea kumfanya apande juu ya mahali pa juu pa dunia,[q]
Hivi kwamba akala mazao ya shamba.[r]
Naye akaendelea kumfanya anyonye asali kutoka katika mwamba,[s]

SURA 32

a Kum 4:26
Kum 30:19
b Ayu 29:22
Isa 55:10
c Met 19:12
Ho 14:5
d Zb 72:6
e Mik 5:7
f Kut 34:5
Zb 105:1
Yoh 17:26
g 1Nya 29:11
Zb 145:3
h 2Sa 22:31
Zb 18:2
Zb 19:7
Yak 1:17
i Zb 33:5
Zb 67:4
Da 4:37
j Kum 7:9
Ne 9:33
Zb 98:3
Ebr 10:23
1Pe 4:19
k Kum 25:16
Ayu 34:10
Ro 3:5
l Mwa 18:25
Zb 92:15
Zb 99:4
Ho 14:9
m Kum 31:27
Amu 2:19
Zb 14:1
n Isa 1:4
Yer 15:6
Yak 1:14
o Zb 78:8
Lu 9:41
Flp 2:15
p Isa 1:2
q Yer 4:22
r Kut 4:22
Kum 32:18
2Sa 7:23
Isa 63:16
s Zb 55:22
t Isa 63:11
u Kut 13:14
Zb 44:1

Safu ya 2

a Zb 78:3
b Mwa 10:5
Zb 115:16
c Mwa 11:9
d Kum 2:5
Kum 2:19
Mdo 17:26
e Mwa 15:18
Kut 23:31
Zb 105:44
f Kut 15:16
Kut 19:5
Kum 7:6
Kum 26:19
g 1Sa 10:1
Zb 74:2
Zb 78:71
h Kum 8:15
Ho 13:5
i Zb 107:4
Yer 2:6
j Ne 9:19
k Ne 9:20
Zb 8:4
l Zb 17:8
Zek 2:8
m Isa 31:5
n Kut 19:4
o Kum 1:31
p Isa 43:12
q Kum 33:29
Isa 58:14
r Kum 8:8

s Zb 81:16.

Na mafuta kutoka katika
jiwe gumu;[a]
14 Siagi ya mifugo na maziwa
ya kundi[b]
Pamoja na mafuta ya
kondoo-dume,
Na kondoo-dume, uzao wa
Bashani, na mbuzi-dume[c]
Pamoja na mafuta ya figo
ya ngano;[d]
Nawe uliendelea kunywa
kama divai damu ya
zabibu.[e]
15 Yeshuruni[f] alipoanza
kunenepa, ndipo akapiga
teke.[g]
Umepata mafuta,
umekuwa mnene,
umeshiba mno.[h]
Basi akamwacha Mungu,
aliyemfanya,[i]
Na kumdharau Mwamba[j]
wa wokovu wake.
16 Walianza kumchochea awe
na wivu[k] kwa miungu
migeni;[l]
Kwa mambo yenye
kuchukiza waliendelea
kumtia uchungu.[m]
17 Waliwatolea dhabihu roho
waovu, wala si Mungu,[n]
Miungu ambayo
hawakuijua,[o]
Mipya iliyokuja hivi
karibuni,[p]
Ambayo mababu zenu
hawakuifahamu.
18 Mwamba aliyekuzaa wewe,
ulimsahau,[q]
Nawe ukaanza
kumwondoa Mungu
katika kumbukumbu,
yule anayekutokeza kwa
uchungu wa kuzaa.[r]
19 Yehova alipoona hilo, ndipo
akawadharau wao,[s]
Kwa sababu ya usumbufu
uliosababishwa na
wanawe na binti zake.

SURA 32

a Ayu 29:6
b Mwa 18:8
c Eze 39:18
d Zb 147:14
e Mwa 49:11
f Kum 33:5
Isa 44:2
g Ho 4:16
h Kum 31:20
Ne 9:25
Zb 73:7
i Isa 1:4
Isa 51:13
Ho 13:6
j 2Sa 22:47
Zb 89:26
Zb 95:1
k 1Fa 14:22
1Ko 10:22
l Amu 2:12
m 2Fa 23:13
Eze 8:17
n Law 17:7
Zb 106:37
1Ko 10:20
o Kum 28:64
p Amu 5:8
q Zb 106:21
Isa 17:10
Yer 2:32
Yer 3:21
r Kum 4:34
s Amu 2:14
Zb 78:59
Zb 106:40

Safu ya 2

a Kum 31:17
Ayu 34:29
Zb 30:7
b Kum 32:5
Isa 65:2
Mt 17:17
c Isa 1:2
Isa 30:9
d Zb 96:5
Isa 44:10
1Ko 8:4
1Ko 10:20
e 1Sa 12:10
1Sa 12:21
1Fa 16:13
Mdo 14:15
f Ho 1:10
Ho 2:23
Ro 9:25
Ro 11:11
1Pe 2:10
g Ro 10:19
h Zb 21:9
Yer 15:14
Omb 4:11
i Amo 9:2
j Sef 3:8
k Hab 3:10
l Law 26:24
Kum 28:15
m Zb 7:13
Eze 5:16
n Kum 28:53
o Kum 28:22
p Kum 28:21
Amo 4:10
q Law 26:22
Yer 15:3
Eze 5:17
r Hes 21:6
Yer 8:17
Amo 9:3
s Yer 9:16
Omb 1:20
t Yer 9:21
Eze 7:15
u 2Nya 36:17

20 Kwa hiyo akasema, ‘Acha
niufiche uso wangu
kutoka kwao,[a]
Acha nione mwisho wao
utakuwaje baadaye.
Kwa maana wao ni kizazi
chenye upotovu,[b]
Wana ambao ndani yao
hamna uaminifu.[c]
21 Wao wamenichochea niwe
na wivu kwa kile
ambacho si mungu;[d]
Wameniudhi kwa sanamu
zao za ubatili;[e]
Na mimi, nitawachochea
wawe na wivu kwa kile
ambacho si kikundi
cha watu;[f]
Kwa taifa jinga
nitawatia uchungu.[g]
22 Kwa maana moto
umewashwa katika
hasira yangu[h]
Nao utateketeza mpaka
katika Kaburi,* mahali
pa chini zaidi,[i]
Nao utateketeza dunia na
mazao yake[j]
Nao utawasha misingi ya
milima.[k]
23 Nitaongeza misiba juu yao;[l]
Mishale yangu nitaitumia
juu yao.[m]
24 Watachoka kutokana na
njaa[n] na kuliwa na
homa kali[o]
Na maangamizi
machungu.[p]
Na meno ya wanyama
nitatuma juu yao,[q]
Kwa sumu ya watambaazi
wa mavumbini.[r]
25 Nje upanga
utawasababishia vifo,[s]
Na ndani woga,[t]
Wa kijana na bikira,[u]

Kum 32:22* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

Anayenyonya pamoja na
mwanamume mwenye
mvi.[a]
26 Ningalikuwa nimesema:
"Nitawatawanya,[b]
Nitalifanya jina lao likome
kutoka katikati ya watu
wanaoweza kufa,"[c]
27 Isingalikuwa kwa sababu
niliogopa usumbufu
kutoka kwa adui,[d]
Kwamba wapinzani wao
wangaliweza kuelewa
vibaya,[e]
Ili waseme: "Mkono wetu
umeshinda,[f]
Na si Yehova aliyefanya
mambo haya yote."[g]
28 Kwa maana wao ni taifa
ambalo juu yake shauri
huangamia,[h]
Na katikati yao hamna
uelewaji.[i]
29 Laiti wangalikuwa
wenye hekima![j] Ndipo
wangalifikiria hili kwa
uzito.[k]
Wangaliufikiria mwisho
wao baadaye.[l]
30 Mmoja angewezaje
kufuatilia elfu,
Na wawili kuwafanya elfu
kumi wakimbie?[m]
Haingewezekana
isipokuwa Mwamba wao
awe amewauza[n]
Na Yehova awe amewatoa.
31 Kwa maana mwamba wao
si kama Mwamba wetu,[o]
Hata ikiwa adui zetu ndio
wangeamua.[p]
32 Kwa maana mzabibu wao
unatoka katika mzabibu
wa Sodoma
Na kutoka katika matuta
ya Gomora.[q]
Zabibu zao ni zabibu za
sumu,
Vishada vyao ni vichungu.[r]

SURA 32

a Omb 2:21
b Law 26:33
Kum 28:25
Eze 20:23
Lu 21:24
c Kum 9:14
d 1Sa 12:22
Eze 20:14
e Kut 32:12
Hes 14:16
f Zb 115:2
Zb 140:8
g Isa 37:24
h Zb 106:13
Zb 107:11
Lu 7:30
i Isa 6:10
Isa 27:11
Mt 13:15
j Zb 81:13
Met 1:5
Met 27:11
k Zb 107:43
Ho 14:9
1Ti 4:15
l Yer 2:19
Omb 1:9
m 2Nya 24:24
Isa 30:17
n Amu 2:14
1Sa 12:9
Zb 44:12
Isa 50:1
o Kut 14:25
1Sa 2:2
p 1Sa 4:8
Ezr 1:3
Da 2:47
q Isa 1:10
Yud 7
r Isa 5:4
Yer 2:21

Safu ya 2

a Zb 58:4
Zb 140:3
b Ho 13:12
Ro 2:5
c Zb 94:1
Nah 1:2
Ro 12:19
Ebr 10:30
d Zb 9:15
Zb 73:18
Isa 8:15
e Yer 10:15
Lu 19:44
f Isa 30:13
Hab 2:3
2Pe 2:3
g Zb 7:8
Zb 96:13
Ebr 10:30
h Amu 2:18
Zb 90:13
Zb 106:45
Zb 135:14
i Amu 10:14
Yer 2:28
j Kum 32:31
k Eze 16:19
1Ko 10:20
l Ho 2:8
1Ko 10:21
m Amu 10:14
n Amo 9:2
o Isa 41:4
Isa 48:12
p Kum 4:35
Isa 45:5
q 1Sa 2:6
2Fa 5:7
Zb 68:20

33 Divai yao ni sumu ya nyoka
wakubwa
Na sumu kali ya swila.[a]
34 Je, sina akiba yake,
Muhuri ukiwa umetiwa
juu yake katika ghala
langu?[b]
35 Kisasi ni changu, na
malipo.[c]
Katika wakati uliowekwa
mguu wao utasogea kwa
kuyumba-yumba,[d]
Kwa maana siku ya maafa
yao iko karibu,[e]
Na matukio yanafanya
haraka kujitayarisha
kwa ajili yao.'[f]
36 Kwa maana Yehova
atawahukumu watu
wake[g]
Naye atajuta juu ya
watumishi wake,[h]
Kwa sababu ataona
kwamba tegemeo
limetoweka
Na aliyeko tu ni mtu asiye
na uwezo na asiye na
thamani.
37 Naye hakika atasema,
'Miungu yao iko wapi,[i]
Mwamba ambaye
walimkimbilia,[j]
38 Iliyokuwa ikila mafuta ya
dhabihu zao,[k]
Ili kunywa divai ya matoleo
yao ya kinywaji?[l]
Na isimame na kuwasaidia
ninyi.[m]
Na iwe mahali pa maficho
kwa ajili yenu.[n]
39 Oneni sasa kwamba
mimi—mimi ndiye[o]
Na hakuna miungu pamoja
nami.[p]
Mimi huua, nami hufanya
hai.[q]

Nimejeruhi vikali,[a] na
mimi—mimi nitaponya,[b]
Na hakuna anayenyakua
kutoka mkononi
mwangu.[c]
40 Kwa maana mimi nainua
mkono wangu kuelekea
mbinguni kwa kiapo,[d]
Nami ninasema: "Kama
nilivyo hai mpaka
wakati usio na
kipimo,"[e]
41 Kwa kweli nikiunoa
upanga wangu
unaometameta,[f]
Na mkono wangu
ushike hukumu,[g]
Nitawalipa kisasi
wapinzani wangu[h]
Na kutoa malipo kwa
wale wanaonichukia
vikali.[i]
42 Nitailewesha mishale
yangu kwa damu,[j]
Nao upanga wangu
utakula nyama,[k]
Kwa damu ya waliouawa
na mateka,
Kwa vichwa vya viongozi
wa adui.'[l]
43 Furahini, enyi mataifa,
pamoja na watu wake,[m]
Kwa maana atalipiza
kisasi damu ya
watumishi wake,[n]
Naye atawalipa kisasi
adui zake[o]
Naye kwa kweli atafanya
upatanisho kwa ajili ya
nchi ya watu wake."

44 Basi Musa akaja na kusema maneno yote ya wimbo huu masikioni mwa watu,[p] yeye na Hoshea mwana wa Nuni.[q] **45** Baada ya Musa kumaliza kuwaambia Israeli wote maneno yote hayo, **46** ndipo akawaambia: "Tieni mioyo yenu katika maneno yote ninayosema kwa kuwaonya ninyi leo,[a] ili muwaamuru wana wenu wawe waangalifu kufanya maneno yote ya sheria hii.[b] **47** Kwa maana hilo si neno lisilo na thamani kwenu,[c] bali linamaanisha uhai wenu,[d] na kwa neno hili mnaweza kurefusha siku zenu juu ya udongo ambao mnavuka Yordani ili kuumiliki."[e]

48 Na Yehova akasema na Musa siku hiyohiyo, na kumwambia: **49** "Panda juu ya mlima huu wa Abarimu,[f] Mlima Nebo,[g] ulio katika nchi ya Moabu, mbele ya Yeriko, nawe uione nchi ya Kanaani, ninayowapa wana wa Israeli wamiliki.[h] **50** Kisha ufe katika mlima utakaopanda, na kukusanywa kwa watu wako,[i] kama vile Haruni ndugu yako aliyokufa katika Mlima Hori[j] na kukusanywa kwa watu wake; **51** Kwa sababu ninyi mlitenda isivyofaa kunielekea mimi[k] katikati ya wana wa Israeli kwenye maji ya Meriba[l] ya Kadeshi katika nyika ya Zini; kwa sababu ninyi hamkunitakasa mimi katikati ya wana wa Israeli.[m] **52** Kwa maana kutoka mbali utaiona nchi, lakini hutaingia katika nchi ninayowapa wana wa Israeli."[n]

33 Sasa hii ndiyo baraka[o] ambayo Musa mtu wa Mungu wa kweli[p] aliwabariki nayo wana wa Israeli kabla ya kifo chake. **2** Naye akasema:

"Yehova—alikuja kutoka
Sinai,[q]
Naye akamulika juu yao
kutoka Seiri.[r]
Aliangaza kutoka katika
eneo lenye milima la
Parani,[s]

SURA 32

a Hes 12:13
2Nya 21:18
b Yer 17:14
Ho 6:1
c Isa 43:13
d Kut 6:8
Isa 45:23
Ebr 6:13
e Zb 90:2
1Ti 1:17
Ufu 10:6
f Zb 7:12
Eze 21:10
g Isa 66:16
Nah 1:3
h Kum 32:35
Isa 1:24
Isa 59:18
Isa 66:6
Nah 1:2
i Kut 20:5
j Kum 32:23
k Isa 34:6
Eze 38:21
l Yos 10:17
Yos 10:26
1Sa 15:33
m Mwa 12:3
1Fa 8:43
Ro 3:29
Ro 15:10
n 2Fa 9:7
Ufu 6:10
o Kum 32:41
Mik 5:15
Lu 21:22
p Kum 31:22
Ufu 15:3
q Hes 11:28
Kum 31:23

Safu ya 2

a Kum 6:6
Kum 11:18
b Kum 6:7
c 2Ti 3:16
Ebr 4:12
d Law 18:5
Kum 30:19
Ro 10:5
e Met 3:2
f Hes 27:12
g Kum 34:1
h Mwa 10:19
Mwa 15:18
Yos 1:3
i Kum 34:5
j Hes 20:28
Hes 33:38
k Hes 20:12
Hes 27:14
l Hes 20:13
m Law 10:3
Law 22:32
Isa 8:13
Mt 6:9
n Hes 27:13
Kum 3:27
Kum 34:4

SURA 33

o Mwa 49:28
Lu 24:50
p Yos 14:6
Zb 90:Uta
q Kut 19:18
r Amu 5:4
s Hab 3:3

Naye alikuwa pamoja na
makumi ya maelfu ya
watakatifu,[a]
Mashujaa wao kwenye
mkono wake wa kuume.[b]
3 Pia alikuwa akiwatunza
kwa upendo watu wake;[c]
Watakatifu wao wote wako
mkononi mwako.[d]
Na wao—wao waliegama
miguuni pako;[e]
Walianza kupokea baadhi
ya maneno yako.[f]
4 (Musa aliweka juu yetu
sheria kuwa amri,[g]
Miliki ya kutaniko la
Yakobo.)[h]
5 Naye akawa mfalme katika
Yeshuruni,[i]
Wakati ambapo walio
vichwa vya watu
walikusanyika pamoja,[j]
Hesabu kamili ya makabila
ya Israeli.[k]
6 Rubeni na aishi wala asife,[l]
Na watu wake wasiwe
wachache."[m]

7 Nayo hii ndiyo iliyokuwa baraka ya Yuda,[n] alipoendelea kusema:

"Usikie, Ee Yehova, sauti ya
Yuda,[o]
Nawe umlete kwa watu
wake.
Mikono yake imeshindania
kilicho chake;
Nawe uwe msaidizi juu ya
wapinzani wake."[p]
8 Na Lawi akamwambia:[q]
"Thumimu yako na Urimu[r]
yako ni vyake mtu aliye
mshikamanifu kwako,[s]
Uliyemjaribu huko Masa.[t]
Ulianza kushindana naye
kando ya maji ya Meriba,[u]
9 Mtu aliyemwambia baba
yake na mama yake,
'Mimi sijamwona.'

SURA 33

a Da 7:10; Ga 3:19; Yud 14
b Zb 68:17
c Kum 7:8; Kum 23:5; Zb 47:4; Ho 11:1
d Kut 19:6; Zb 50:5
e Kut 19:23
f Kut 20:19
g Kut 24:8; Yoh 1:17; Mdo 15:5; 1Ko 9:9
h Kum 4:8; Mdo 7:53
i Kum 32:15; Isa 44:2
j Kut 18:25; Kut 19:7; Hes 1:44
k Hes 1:46
l Mwa 49:3; Yos 22:1; 1Nya 5:1
m Hes 26:7; Yos 13:15
n Mwa 49:8; 1Nya 5:2
o Zb 78:68
p Amu 1:2; 2Sa 7:1; 2Sa 7:9
q Mwa 49:5; Hes 3:12; Hes 18:24
r Kut 28:30; Law 8:8; Ezr 2:63
s Kut 32:26; Ebr 7:26
t Kut 17:7; Kum 6:16
u Hes 20:13

Safu ya 2

a Kut 32:27; Law 10:6
b Law 10:7
c Mal 2:5
d Law 10:11; Kum 17:9; Yer 18:18
e 2Nya 15:3; 2Nya 17:9; Mal 2:7
f Kut 30:7; Hes 16:40
g Law 1:9; Zb 51:19
h Zb 18:32; Isa 40:29; Hab 3:19; Flp 4:13
i Kum 18:5; Mal 2:6
j Mdo 23:4
k Zb 3:7; Amo 5:10
l Mwa 49:27
m 2Sa 7:16
n Zb 4:8
o Yos 18:11; Zb 68:27
p Yos 18:28; Amu 1:21; 2Sa 5:9; Zb 125:2
q Mwa 49:22
r Yos 16:1; Met 10:22
s Mwa 27:28; Zek 8:12
t Mwa 49:25

Hata ndugu zake
hakuwatambua,[a]
Na wanawe hakuwajua.
Kwa maana walilishika
neno lako,[b]
Na agano lako waliendelea
kulishika.[c]
10 Na wamfundishe Yakobo
hukumu zako[d]
Na Israeli sheria yako.[e]
Na watoe uvumba mbele za
mianzi ya pua yako[f]
Na toleo zima kwenye
madhabahu yako.[g]
11 Bariki, Ee Yehova, nguvu
zake,[h]
Na ufurahie utendaji wa
mikono yake.[i]
Waumize vikali viunoni
mwao wale wanaoinuka
juu yake,[j]
Na wale wanaomchukia
vikali, ili wasiinuke."[k]
12 Na Benyamini
akamwambia:[l]
"Mpendwa[m] wa Yehova
na akae katika usalama
kando yake,[n]
Anapomkinga siku nzima,[o]
Naye lazima akae katikati
ya mabega yake."[p]
13 Na Yosefu akamwambia:[q]
"Nchi yake na ibarikiwe
daima na Yehova[r]
Kwa vitu bora vya
mbinguni, kwa umande,[s]
Na kwa kilindi cha maji
kilicho chini,[t]
14 Na kwa vitu bora, mazao ya
jua,[u]
Na kwa vitu bora, mazao ya
mwezi.[v]
15 Na kwa vilivyo bora kabisa
kutoka katika milima ya
mashariki,[w]

u 2Sa 23:4; v Law 26:5; Zb 65:9; w Mwa 37:25; Yos 17:18.

Na kwa vitu bora vya
vilima vyenye kudumu
mpaka wakati usio na
kipimo,
16 Na kwa vitu bora vya dunia
na vitu vinavyoijaza,[a]
Na kwa kibali cha Yule
anayekaa katika kichaka
cha miiba.[b]
Na vije juu ya kichwa cha
Yosefu[c]
Na juu ya utosi wa kichwa
cha yule aliyechaguliwa
kutoka kati ya ndugu
zake.[d]
17 Kama mzaliwa wa kwanza
wa ng'ombe-dume ndivyo
fahari yake ilivyo,[e]
Na pembe zake ni pembe
za ng'ombe-dume wa
mwituni.[f]
Atasukuma vikundi vya
watu kwa pembe hizo[g]
Wote pamoja mpaka
miisho ya dunia,
Nao ni makumi ya maelfu
ya Efraimu,[h]
Nao ni maelfu ya Manase."
18 Naye akamwambia
Zabuloni:[i]
"Shangilia, Ee Zabuloni,
kwa sababu ya kutoka
kwako nje,[j]
Na, Isakari, kwa sababu ya
mahema yako.[k]
19 Wataita vikundi vya watu
mlimani.
Huko watatoa dhabihu za
uadilifu.[l]
Kwa maana watanyonya
mali nyingi ya bahari[m]
Na akiba zilizofichika za
mchanga."
20 Naye akamwambia Gadi:[n]
"Amebarikiwa yule
anayepanua mipaka ya
Gadi.[o]

SURA 33

a Kum 8:8
Zb 24:1
b Kut 3:4
Mdo 7:30
c Mwa 49:26
1Nya 5:1
d Mwa 37:7
1Nya 5:2
e Yos 17:1
f Zb 22:21
Zb 92:10
g 1Fa 22:11
Zb 44:5
h Mwa 48:19
i Mwa 49:13
j Yos 19:10
Amu 5:14
k Mwa 49:14
Yos 19:17
l Zb 4:5
m Mwa 49:13
Mt 4:13
n Mwa 49:19
o Yos 13:8
Yos 13:24

Safu ya 2

a 1Nya 12:8
Met 28:1
b 1Nya 5:18
1Nya 5:20
c Hes 32:1
d Hes 32:21
Hes 32:27
Hes 32:33
Yos 1:14
Yos 1:15
Yos 4:12
Yos 22:1
e Mwa 49:16
f Amu 13:2
Amu 13:24
Amu 15:8
Amu 15:20
Amu 16:30
g Yos 19:47
Amu 18:27
Amu 18:29
1Nya 12:35
h Mwa 49:21
i Yos 19:32
j Mwa 49:20
k Zb 127:3
Zb 128:3
l Met 3:4
m Kum 32:13
Ayu 29:6
n Kum 8:9
o Kut 15:11
Zb 86:8
Zb 89:6
Yer 10:6
p Kum 32:15
Kum 33:5
Isa 44:2
q Zb 68:33
r Zb 68:34
Zb 93:1
Zb 104:3
s Zb 46:11
Zb 90:1
Zb 91:2
Zb 125:2

Yeye atakaa kama simba,[a]
Naye atararua mkono,
naam, utosi wa kichwa.[b]
21 Naye atajichagulia sehemu
ya kwanza,[c]
Kwa maana huko fungu la
mpaji-sheria
linahifadhiwa.[d]
Na walio vichwa vya watu
watajikusanya pamoja.
Hakika atautimiza uadilifu
wa Yehova
Na maamuzi yake ya
hukumu pamoja na
Israeli."
22 Naye akamwambia Dani:[e]
"Dani ni mwana-simba.[f]
Ataruka kutoka Bashani."[g]
23 Naye akamwambia
Naftali:[h]
"Naftali ameshiba kibali
Naye amejaa baraka ya
Yehova.
Miliki magharibi na
kusini."[i]
24 Naye akamwambia Asheri:[j]
"Aliyebarikiwa na wana ni
Asheri.[k]
Na awe aliyekubaliwa na
ndugu zake,[l]
Na yule anayechovya mguu
wake katika mafuta.[m]
25 Chuma na shaba ni
makufuli ya lango lako,[n]
Na kulingana na siku
zako ndivyo yalivyo
matembezi yako ya
starehe.
26 Hakuna aliye kama Mungu
wa kweli[o] wa Yeshuruni,[p]
Anayepanda juu ya mbingu
ili kukusaidia[q]
Na juu ya anga zenye
kutanda mawingu katika
adhama yake.[r]
27 Mungu wa nyakati za kale
ni mahali pa kujificha,[s]

Na chini kuna mikono
yenye kudumu mpaka
wakati usio na kipimo.[a]
Naye atawafukuzia mbali
adui zako toka mbele
yako,[b]
Naye atasema,
'Waangamize!'[c]
28 Na Israeli atakaa katika
usalama,[d]
Chemchemi ya Yakobo
peke yake,[e]
Katika nchi ya nafaka na
divai mpya.[f]
Naam, mbingu zake
zitatiririsha umande.[g]
29 Una furaha, Ee Israeli![h]
Ni nani aliye kama wewe,[i]
Kikundi cha watu
kinachofurahia wokovu
wa Yehova,[j]
Aliye ngao ya msaada
wako,[k]
Na Yule aliye upanga wako
wa adhama?[l]
Kwa hiyo adui zako
watatetemeka mbele
yako,[m]
Na wewe—utapakanyaga
mahali pao pa juu."[n]

34 Kisha Musa akatoka katika nchi tambarare za jangwa la Moabu na kuingia katika Mlima Nebo,[o] mpaka juu ya Pisga,[p] mbele ya Yeriko.[q] Naye Yehova akamwonyesha nchi yote, Gileadi mpaka Dani,[r] **2** na Naftali yote na nchi ya Efraimu na Manase na nchi yote ya Yuda mpaka bahari ya magharibi,[s] **3** na Negebu[t] na Wilaya,[u] nchi tambarare ya bonde la Yeriko, jiji la mitende,[v] mpaka Soari.[w]

4 Na Yehova akamwambia: "Hii ndiyo nchi ambayo nilimwapia Abrahamu, Isaka na Yakobo, na kusema, 'Nitaupa uzao wako.'[a] Nimekufanya uione kwa macho yako mwenyewe, kwa maana wewe hutavuka kuingia huko."[b]

5 Baada ya hilo Musa mtumishi wa Yehova[c] akafa huko katika nchi ya Moabu kulingana na agizo la Yehova.[d] **6** Naye akamzika katika bonde katika nchi ya Moabu mbele ya Bethpeori,[e] na hakuna mtu ambaye amepata kujua kaburi lake mpaka leo hii.[f] **7** Naye Musa alikuwa na umri wa miaka 120 wakati wa kifo chake.[g] Jicho lake halikuwa limeingia giza,[h] na nguvu zake hazikuwa zimepotea.[i] **8** Na wana wa Israeli wakamlilia Musa kwenye nchi tambarare za jangwa la Moabu kwa siku 30.[j] Mwishowe siku za kulia za kipindi cha kumwombolezea Musa zikamalizika.

9 Na Yoshua mwana wa Nuni alikuwa amejaa roho ya hekima,[k] kwa kuwa Musa alikuwa ameweka mkono wake juu yake;[l] na wana wa Israeli wakaanza kumsikiliza nao wakafanya kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.[m] **10** Lakini hajainuka kamwe nabii katika Israeli aliye kama Musa,[n] ambaye Yehova alimjua uso kwa uso,[o] **11** kuhusiana na ishara zote na miujiza yote ambayo Yehova alimtuma afanye katika nchi ya Misri kwa Farao na watumishi wake wote na nchi yake yote,[p] **12** na kuhusiana na mkono wote wenye nguvu na hofu kuu yote ambayo Musa alifanya ionekane mbele ya macho ya Israeli wote.[q]

SURA 33
a Isa 40:11; Ho 11:3
b Kum 9:3
c Kum 31:4
d Yer 23:6; Yer 33:16
e Zb 68:26; Isa 48:1
f Kum 8:8
g Kum 11:11; Kum 33:13
h Zb 33:12; Zb 144:15; Zb 146:5
i Kum 4:7; 2Sa 7:23; Zb 147:20
j Zb 27:1; Isa 12:2
k Mwa 15:1; Zb 115:9
l Amu 7:20
m 2Sa 22:45; Zb 66:3; Zb 81:15
n Kum 32:13

SURA 34
o Hes 27:12; Kum 32:49
p Hes 21:20; Kum 3:27
q Hes 36:13
r Yos 19:47; Amu 18:29
s Kut 23:31; Hes 34:6; Kum 11:24
t Yos 15:1
u Mwa 13:10; 1Fa 7:46
v 2Nya 28:15
w Mwa 19:22; Isa 15:5

Safu ya 2
a Mwa 12:7; Mwa 26:3; Mwa 28:13
b Hes 20:12; Kum 32:52
c Hes 12:7; Mal 4:4
d Kum 32:50; Yos 1:2
e Kum 3:29
f Mdo 2:31; Yud 9
g Kum 31:2; Mdo 7:23; Mdo 7:30; Mdo 7:36
h Mwa 27:1; Mwa 48:10
i Yos 14:11
j Hes 20:29
k Amu 3:10; Amu 6:34; 1Fa 3:12
l Hes 27:18; Kum 31:14; Mdo 6:6; 1Ti 4:14
m Hes 27:21; Yos 1:16; Ebr 13:17
n Kum 18:15; Mdo 3:22; Mdo 7:37
o Kut 33:11; Kut 33:20; Hes 12:8
p Kum 4:34; Zb 78:43
q Kut 3:19; Kum 26:8; Lu 24:19.

YOSHUA

1 Basi ikawa kwamba baada ya kifo cha Musa mtumishi wa Yehova, Yehova akamwambia Yoshua[a] mwana wa Nuni, mhudumu[b] wa Musa: **2** "Musa mtumishi wangu amekufa;[c] basi simama sasa, vuka huu mto Yordani, wewe na watu hawa wote, mwingie katika nchi ambayo ninawapa wao, wana wa Israeli.[d] **3** Kila mahali ambapo wayo wa mguu wenu utakanyaga, nitawapa ninyi mahali hapo, kama vile nilivyomwahidi Musa.[e] **4** Na eneo lenu litakuwa kutoka nyika hii na huu mlima Lebanoni mpaka ule mto mkubwa, mto Efrati, yaani, nchi yote ya Wahiti,[f] na mpaka kwenye ile Bahari Kuu upande wa magharibi.[g] **5** Hakuna yeyote atakayesimama imara mbele yako siku zote za maisha yako.[h] Nitakuwa pamoja nawe,[i] kama vile nilivyokuwa pamoja na Musa. Sitakutupa wala kukuacha kabisa.[j] **6** Uwe hodari na mwenye nguvu,[k] kwa maana ni wewe utakayewafanya watu hawa wairithi[l] ile nchi ambayo niliwaapia mababu zao kuwa nitawapa.[m]

7 "Ila tu uwe hodari na mwenye nguvu sana ili uangalie kufanya kulingana na sheria yote ambayo Musa mtumishi wangu alikuamuru.[n] Usiiache, kwenda upande wa kuume wala wa kushoto,[o] kusudi utende kwa hekima kila mahali unapoenda.[p] **8** Kitabu hiki cha sheria kisiondoke katika kinywa chako,[q] nawe ukisome kwa sauti ya chini mchana na usiku, upate kuangalia kufanya kulingana na yote ambayo yameandikwa ndani yake;[a] kwa maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha utatenda kwa hekima.[b] **9** Je, mimi sikukuamuru wewe?[c] Uwe hodari na mwenye nguvu. Usitetemeke wala usiwe na hofu,[d] kwa maana Yehova Mungu wako yupo pamoja nawe kila mahali unapoenda."[e]

10 Ndipo Yoshua akawaamuru maofisa wa watu, akisema: **11** "Piteni katikati ya kambi na kuwaamuru watu, mkisema, 'Jitayarishieni chakula, kwa kuwa siku tatu kutoka sasa mtavuka huu mto Yordani ili kuingia na kuimiliki nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa ninyi mpate kuimiliki.'"[f]

12 Kisha Yoshua akawaambia Warubeni na Wagadi na nusu ya kabila la Manase: **13** "Kumbukeni neno lile ambalo Musa mtumishi wa Yehova aliwaamuru,[g] akisema, 'Yehova Mungu wenu anawapa ninyi pumziko naye amewapa nchi hii. **14** Wake zenu, watoto wenu wadogo na mifugo yenu, watakaa katika nchi ambayo Musa amewapa ninyi ng'ambo hii ya Yordani;[h] lakini ninyi wanaume mtavuka mkiwa mmejipanga kivita[i] mbele ya ndugu zenu, wanaume wote ambao ni mashujaa wenye nguvu,[j] nanyi mtawasaidia. **15** Kwanza Yehova atakapowapa ndugu zenu pumziko kama vile alivyowapa ninyi, nao pia wawe wameirithi nchi ambayo Yehova Mungu wenu anawapa,[k] ndipo mtakaporudi katika nchi ya urithi wenu na kuimiliki,[l] nchi ile ambayo Musa mtumishi wa Yehova amewapa ng'ambo ya Yordani upande wa mashariki.'"[m]

SURA 1

a Kum 31:14
b Kut 24:13
Hes 11:28
c Kum 34:5
d Hes 27:21
Kum 3:28
e Kum 11:24
f Hes 13:29
Yos 11:3
g Mwa 15:18
Kut 23:31
Hes 34:3
Kum 1:7
Yos 15:4
h Kum 7:24
Kum 11:25
Ro 8:31
i Kut 3:12
Yos 3:7
j Kum 31:6
Ebr 13:5
k Kum 1:38
Kum 31:23
Zb 27:14
l Hes 34:17
m Mwa 12:7
Mwa 15:18
Mwa 26:3
n Kum 31:7
o Kum 5:32
Kum 28:14
p Kum 29:9
1Fa 2:3
q Kum 6:6
Kum 30:14

Safu ya 2

a Kum 17:19
Zb 1:2
1Ti 4:15
Yak 1:25
b 1Nya 22:13
c Kum 31:7
d Kum 31:8
Yos 8:1
e Kut 23:27
Zb 46:7
f Kum 9:1
Kum 11:31
Yos 3:2
g Hes 32:20
Yos 22:2
h Kum 3:19
Kum 29:8
Yos 13:8
i Kut 13:18
Hes 32:21
Kum 3:18
j Hes 1:3
Hes 26:2
k Hes 32:17
Hes 32:22
Kum 3:20
l Yos 22:4
m Hes 32:33
Yos 22:9

16 Basi wakamjibu Yoshua, wakisema: "Yote ambayo umetuamuru tutafanya, na popote utakapotutuma tutaenda.[a] **17** Kama vile tulivyomsikiliza Musa katika kila jambo, ndivyo tutakavyokusikiliza wewe. Ila tu Yehova Mungu wako na awe pamoja nawe[b] kama vile alivyokuwa pamoja na Musa.[c] **18** Mtu yeyote atakayeasi agizo lako,[d] akatae kuyasikiliza maneno yako katika mambo yote ambayo utamwamuru, atauawa.[e] Ila tu uwe hodari na mwenye nguvu."[f]

2 Kisha Yoshua mwana wa Nuni akatuma kisiri wanaume wawili kutoka Shitimu,[g] waende wakiwa wapelelezi, akawaambia: "Nendeni, angalieni nchi na Yeriko." Basi wakaenda wakafika nyumbani kwa mwanamke mmoja kahaba ambaye jina lake lilikuwa Rahabu,[h] nao wakakaa humo. **2** Baada ya muda mfalme wa Yeriko akaambiwa hivi: "Tazama! Wanaume kutoka kwa wana wa Israeli wameingia humu leo usiku ili kupeleleza nchi." **3** Ndipo mfalme wa Yeriko akatuma watu kwa Rahabu, akisema: "Watoe nje wale wanaume waliokuja kwako, walioingia katika nyumba yako, kwa maana wamekuja kwa kusudi la kupeleleza nchi nzima."[i]

4 Wakati huohuo mwanamke huyo akawachukua wale wanaume wawili, akawaficha. Kisha akasema: "Ni kweli, wanaume hao walikuja kwangu, lakini sikujua walikotoka. **5** Ikawa wakati wa kufungwa kwa lango,[j] kulipokuwa na giza, wanaume wale wakatoka. Wala sijui walikokwenda. Wafuatilieni haraka, kwa maana mtawafikia." **6** (Lakini alikuwa amewapandisha darini,[a] naye akawaficha kati ya majani ya kitani yaliyokuwa yametandikwa kwa mistari kwa ajili yake juu ya dari.) **7** Basi watu hao wakawafuatilia kuelekea upande wa Yordani vivukoni,[b] nao wakalifunga lango mara moja baada ya wale waliowafuatilia kuondoka.

8 Kabla hawajalala akaenda kwao juu ya dari. **9** Naye akawaambia wanaume hao: "Najua hakika ya kwamba Yehova atawapa nchi hii,[c] na ya kwamba tumeshikwa na hofu kwa sababu yenu,[d] na ya kwamba wakaaji wote wa nchi wamevunjika moyo kwa sababu yenu.[e] **10** Kwa maana tumesikia jinsi ambavyo Yehova aliyakausha maji ya Bahari Nyekundu mbele yenu wakati mlipotoka Misri,[f] na yale mliyowatendea wale wafalme wawili wa Waamori waliokuwa ng'ambo ile nyingine ya Yordani, yaani, Sihoni[g] na Ogu,[h] ambao mliwaangamiza.[i] **11** Tuliposikia hayo, ndipo mioyo yetu ikaanza kuyeyuka,[j] wala roho yoyote haijaamka bado ndani ya mtu yeyote kwa sababu yenu,[k] kwa kuwa Yehova Mungu wenu ni Mungu juu mbinguni na chini duniani.[l] **12** Basi sasa, tafadhali, niapieni kwa Yehova[m] kwamba, kwa kuwa nimewatendea ninyi fadhili zenye upendo, ninyi pia kwa hakika mtaitendea nyumba ya baba yangu[n] kwa fadhili zenye upendo, tena mnipe ishara[o] yenye kuaminika. **13** Nanyi mtawahifadhi hai baba yangu[p] na mama yangu na ndugu zangu na dada zangu na watu wao wote, nanyi mtazikomboa nafsi zetu kutoka katika kifo."[q]

14 Ndipo wanaume hao wakamwambia: "Nafsi zetu na zife badala yenu![r] Ikiwa hamtasema

SURA 1
a Hes 32:25; Ebr 13:17
b 1Sa 16:18; 1Sa 17:37
c Hes 27:20; Kum 34:9
d 1Sa 12:15; 1Sa 15:23; Met 17:11
e Kum 17:12; 1Sa 11:12
f Kum 31:7; Yos 1:6

SURA 2
g Hes 25:1; Hes 33:49
h Yos 6:17; Mt 1:5; Ebr 11:31; Yak 2:25
i Mwa 42:9; 2Sa 10:3
j Ne 13:19

Safu ya 2
a Kum 22:8; 2Sa 11:2; Mdo 10:9
b Amu 3:28; Amu 12:5
c Mwa 13:15; Mwa 15:18; Kut 3:8
d Kut 23:27; Kum 2:25; Kum 11:25
e Kut 15:15; Yos 5:1; Zb 112:10
f Kut 14:21; Kut 15:14; Yos 4:23; Yos 9:9
g Hes 21:21; Hes 21:24
h Hes 21:34; Kum 3:3; Yos 9:10; Zb 135:11
i Law 27:29
j Yos 5:1
k Kut 15:15
l Kum 4:39; 2Nya 20:6; Zb 83:18; Zb 135:6; Da 4:35
m Kum 10:20
n Est 8:6
o Kut 12:13; Yos 2:18; Amu 6:17
p Efe 6:2
q Yos 6:23
r Hes 30:2; Mt 5:33

juu ya hii shughuli yetu, itatukia kwamba wakati Yehova atakapotupa nchi hii, sisi pia tutakutendea kwa fadhili zenye upendo na kwa uaminifu."[a] **15** Baada ya hayo akawashusha kwa kamba kupitia dirishani, kwa kuwa nyumba yake ilikuwa upande wa ukuta, naye alikuwa akikaa ukutani.[b] **16** Naye akawaambia: "Nendeni katika eneo lenye milima, ili wale wanaowafuatilia wasije wakawapata; nanyi mjifiche huko siku tatu, mpaka wale wanaowafuatilia wawe wamerudi, kisha mwende zenu baadaye."

17 Nao wale wanaume wakamwambia: "Hatuna hatia kuhusiana na kiapo chako hiki ambacho umetuapisha.[c] **18** Tazama! Tutaingia katika nchi hii. Funga kamba hii ya uzi mwekundu katika dirisha ambalo ulitushushia, na baba yako na mama yako na ndugu zako na nyumba yote ya baba yako uwakusanye kwako ndani ya nyumba.[d] **19** Na itatukia kwamba mtu yeyote atakayeondoka katika milango ya nyumba yako na kwenda nje,[e] damu yake itakuwa juu ya kichwa chake mwenyewe, nasi hatutakuwa na hatia; na kila mtu atakayeendelea kukaa nawe ndani ya nyumba, damu yake itakuwa juu ya vichwa vyetu ikiwa mkono utanyooshwa juu yake. **20** Nawe ukitoa habari ya hii shughuli yetu,[f] sisi pia hatutakuwa na hatia kuhusiana na hiki kiapo chako ulichotuapisha." **21** Naye akasema: "Na iwe hivyo kulingana na maneno yenu."

Kwa hiyo akawaacha waende, nao wakaenda zao. Kisha akafunga ile kamba nyekundu dirishani. **22** Basi wakaenda na kufika katika eneo lenye milima, wakakaa huko siku tatu, mpaka wale wenye kuwafuatilia walipokuwa wamerudi. Basi wale wenye kuwafuatilia walikuwa wakiwatafuta katika kila barabara, lakini hawakuwaona. **23** Kisha wale wanaume wawili wakashuka tena kutoka katika eneo lenye milima, wakavuka na kwenda kwa Yoshua mwana wa Nuni, nao wakaanza kumweleza mambo yote yaliyowapata. **24** Nao wakamwambia Yoshua: "Yehova ameitia nchi yote mkononi mwetu.[a] Na kwa hiyo wakaaji wote wa nchi wamevunjika moyo pia kwa sababu yetu."[b]

3 Ndipo Yoshua akaamka asubuhi na mapema, yeye pamoja na wana wote wa Israeli wakaanza safari kutoka Shitimu,[c] wakafika Yordani; nao wakalala hapo usiku kucha kabla ya kuvuka.

2 Basi ikawa mwishoni mwa siku tatu,[d] maofisa[e] wakapita katikati ya kambi **3** wakawaamuru watu, wakisema: "Mara mtakapoliona sanduku la agano la Yehova Mungu wenu, na makuhani Walawi wakiwa wamelichukua,[f] ndipo mtakapoondoka mahali penu, nanyi mlifuate, **4** —ila mwache kuwe na umbali wa karibu kipimo cha mikono elfu mbili kati yenu na sanduku hilo;[g] msilikaribie—ili mpate kujua njia mnayopaswa kutembea, kwa maana hamjapata kuipita njia hiyo hapo mbeleni."

5 Sasa Yoshua akawaambia watu: "Jitakaseni,[h] kwa maana kesho Yehova atafanya mambo ya ajabu katikati yenu."[i]

6 Kisha Yoshua akawaambia makuhani: "Chukueni sanduku la agano,[j] na mpite mbele ya watu." Basi wakachukua sanduku la agano, wakapita mbele ya watu.

SURA 2

a Amu 1:24
1Sa 30:15
Mt 10:41

b Ebr 11:31

c Hes 30:2

d Yos 6:23
Est 8:6

e Hes 35:26

f Yos 2:14

Safu ya 2

a Kut 23:31
Yos 6:2
Yos 21:44
Ne 9:24

b Kut 15:15
Yos 2:9
Yos 2:11
Yos 5:1

SURA 3

c Hes 25:1
Yos 2:1

d Yos 1:11

e Kum 1:15
Kum 20:5
Kum 31:28
Yos 1:10

f Hes 4:15
Kum 31:9
1Nya 15:2

g Kut 19:12

h Kut 19:10
Law 20:7

i Kut 34:10
Zb 72:18
Zb 86:10

j Kut 25:10
Hes 4:15

7 Ndipo Yehova akamwambia
Yoshua: "Leo nitaanza kukufa-
nya uwe mkuu machoni pa Isra-
eli wote,[a] ili wajue kwamba ni-
takuwa pamoja nawe[b] kama vile
nilivyokuwa pamoja na Musa.[c]
8 Na wewe—waamuru[d] maku-
hani wanaolichukua sanduku
la agano, ukisema, 'Mara mtaka-
pofika kwenye ukingo wa maji
ya Yordani, simameni[e] katika
Yordani.'"

9 Ndipo Yoshua akaendelea
kuwaambia wana wa Israeli:
"Karibieni hapa, msikilize ma-
neno ya Yehova Mungu wenu."
10 Kisha Yoshua akasema:
"Kwa jambo hili mtajua kwa-
mba Mungu aliye hai yupo ka-
tikati yenu,[f] na kwamba bila
shaka atawafukuzia mbali kuto-
ka mbele yenu Wakanaani na
Wahiti na Wahivi na Waperizi
na Wagirgashi na Waamori na
Wayebusi.[g] **11** Tazameni! san-
duku la agano la Bwana wa du-
nia yote linapita mbele yenu ku-
ingia Yordani. **12** Basi sasa ji-
chukulieni wanaume kumi na
wawili kutoka katika makabi-
la ya Israeli, kila kabila mwana-
mume mmoja.[h] **13** Na itatukia
kwamba mara tu nyayo za mi-
guu ya makuhani wanaolichu-
kua sanduku la Yehova, Bwana
wa dunia yote, zitakapokanya-
ga maji ya Yordani, maji ya Yor-
dani yatazuiliwa, maji yanayo-
shuka kutoka juu, nayo yatasi-
mama kama ukuta wa maji."[i]

14 Basi ikawa watu walipoto-
ka katika mahema yao kab-
la tu ya kuvuka Yordani, nao
makuhani wakiwa wamelichu-
kua sanduku[j] la agano mbe-
le ya watu, **15** mara tu wachu-
kuaji wa lile Sanduku walipo-
fika Yordani na miguu ya ma-
kuhani waliolichukua Sanduku
ilipotumbukizwa katika maji ya
ukingoni (maana Yordani hu-
furika kingo[a] zake zote siku
zote za mavuno), **16** ndipo
maji yanayoshuka kutoka juu
yakaanza kusimama. Yakasima-
ma kama ukuta wa maji[b] mba-
li sana huko Adamu, jiji lililo
kando ya Sarethani,[c] na yale ya-
nayoshuka kuelekea bahari ya
Araba, yaani, Bahari ya Chu-
mvi,[d] yakaisha. Yalizuiliwa ka-
bisa, na watu wakavuka mbe-
le ya Yeriko. **17** Wakati huo-
huo wale makuhani waliolichu-
kua sanduku la agano la Yehova
wakaendelea kusimama bila ku-
songa kwenye nchi kavu[e] katika-
ti ya Yordani, huku Israeli wote
wakivuka juu ya nchi kavu,[f]
mpaka taifa zima lilipokuwa li-
memaliza kuvuka Yordani.

4 Kisha ikawa kwamba mara
tu taifa zima lilipokuwa
limemaliza kuvuka Yordani,[g]
Yehova akamwambia Yoshua:
2 "Jichukulieni wanaume kumi
na wawili kutoka kati ya watu,
kila kabila mwanamume mmo-
ja,[h] **3** na kuwaamuru, mkise-
ma, 'Jichukulieni mawe kumi
na mawili[i] kutoka katikati ya
Yordani, kutoka mahali amba-
po miguu ya makuhani ilisima-
ma,[j] nanyi myachukue na ku-
yaweka katika makao[k] mtaka-
yokaa usiku huu.'"

4 Basi Yoshua akawaita wa-
naume kumi na wawili[l] ambao
alikuwa amechagua kutoka
kati ya wana wa Israeli, kila
kabila mwanamume mmoja;
5 kisha Yoshua akawaambia:
"Piteni mbele ya sanduku la Ye-
hova Mungu wenu mpaka kati-
kati ya Yordani, na mjichuku-
lie kila mmoja wenu jiwe moja
begani mwake, kulingana na
hesabu ya makabila ya wana wa
Israeli, **6** ili kwamba jambo
hili liwe ishara katikati yenu.[m]

SURA 3
a Yos 4:14
b Kum 31:8; Yos 1:5; Yos 1:17
c Kut 3:12; Kut 14:31
d Yos 1:18
e Yos 3:17
f Kut 17:7; Law 26:11; Hes 11:20; Kum 7:21
g Kut 3:8; Kum 7:1; Zb 24:1; Zb 44:2; Zek 4:14
h Yos 4:2
i Kut 15:8; Zb 114:3
j Kut 25:10; Yos 3:6; Mdo 7:45

Safu ya 2
a Yos 4:18; 1Nya 12:15
b Yos 3:13
c 1Fa 7:46
d Mwa 14:3; Hes 34:3; Kum 3:17; Yos 12:3
e Yos 4:3; 2Fa 2:8
f Zb 66:6

SURA 4
g Hes 14:29; Hes 26:51; Hes 26:65
h Yos 3:12
i Kum 27:2
j Yos 3:17
k Yos 4:19; Yos 4:20
l Yos 3:12
m Mwa 31:45

Ikiwa wana wenu watauliza
wakati ujao, wakisema, 'Kwa
nini mna mawe haya?'[a] **7** Ndi-
po mtakapowaambia, 'Kwa sa-
babu maji ya Yordani yalizuili-
wa kabisa kutoka mbele ya san-
duku la agano la Yehova.[b] Lili-
popita kati ya Yordani, maji ya
Yordani yalizuiliwa kabisa, na
mawe haya yatakuwa ukumbu-
sho kwa wana wa Israeli mpaka
wakati usio na kipimo.'"[c]
8 Basi wana wa Israeli waka-
fanya hivyo, kama vile Yoshua
alivyokuwa ameamuru, nao wa-
kachukua mawe kumi na mawi-
li kutoka katikati ya Yordani,
kama vile Yehova alivyokuwa
amemwambia Yoshua, ili yali-
ngane na hesabu ya makabila ya
wana wa Israeli;[d] nao wakaya-
chukua na kuyapeleka kwenye
yale makao[e] na kuyaweka huko.
9 Pia kulikuwa na mawe
kumi na mawili ambayo Yoshua
alipanga katikati ya Yordani ka-
tika mahali pale iliposimama[f]
miguu ya wale makuhani walio-
chukua sanduku la agano, nayo
yangali hapo mpaka leo hii.
10 Na wale makuhani wali-
olichukua Sanduku walikuwa
wamesimama katikati[g] ya Yor-
dani mpaka shughuli hiyo yote
ambayo Yehova alikuwa ame-
mwamuru Yoshua awaambie
watu ilipomalizika, kulinga-
na na yote ambayo Musa aliku-
wa amemwamuru Yoshua.[h] Na
wakati huo wote watu wa-
kafanya haraka[i] na kuvuka.
11 Kisha ikawa kwamba mara
tu watu wote walipokuwa wa-
memaliza kuvuka, sanduku[j] la
Yehova likavuka, na hao maku-
hani, mbele ya watu. **12** Ki-
sha wana wa Rubeni na wana
wa Gadi na nusu ya kabila
la Manase[k] wakavuka wakiwa
wamejipanga kivita[l] macho-
ni pa wana wa Israeli, kama
vile Musa alivyokuwa amewaa-
mbia.[a] **13** Karibu watu 40,000
waliotayarishwa kijeshi waka-
vuka mbele za Yehova kwa ajili
ya vita kwenda katika nchi ta-
mbarare za jangwa la Yeriko.
14 Siku hiyo Yehova alimfa-
nya Yoshua kuwa mkuu macho-
ni pa Israeli wote,[b] nao waka-
anza kumwogopa kama vile wa-
livyokuwa wakimwogopa Musa
siku zote za maisha yake.[c]
15 Ndipo Yehova akamwa-
mbia Yoshua: **16** "Waamuru
makuhani wanaochukua san-
duku la ushuhuda[d] kwamba
wapande kutoka ndani ya Yor-
dani." **17** Basi Yoshua aka-
waamuru makuhani, akisema:
"Pandeni kutoka ndani ya Yor-
dani." **18** Kisha ikawa kwa-
mba makuhani waliolichukua
sanduku[e] la agano la Yehova
walipopanda kutoka katikati
ya Yordani nao makuhani waka-
inua miguu[f] yao na kukanyaga
kwenye nchi kavu, ndipo maji
ya Yordani yakaanza kurudi
mahali pake na kufanya kingo
zake zote zifurike[g] kama hapo
mwanzoni.
19 Na watu hao wakapanda
kutoka katika Yordani siku ya
kumi ya mwezi wa kwanza, wa-
kapiga kambi kule Gilgali[h] kwe-
nye mpaka wa mashariki wa
Yeriko.
20 Kisha Yoshua akapanga
katika Gilgali yale mawe kumi
na mawili, ambayo walikuwa wa-
mechukua kutoka katika Yor-
dani.[i] **21** Naye akawaambia
wana wa Israeli: "Wana wenu wa-
takapowauliza baba zao wakati
ujao, wakisema, 'Mawe haya ya-
namaanisha nini?'[j] **22** Ndipo
mtakapowajulisha wana wenu,
mkisema, 'Israeli walivuka huu
mto Yordani ukiwa nchi kavu,[k]

SURA 4

a Kut 12:26
Kut 13:14
Kum 6:20
Yos 4:21
Zb 78:3
Isa 38:19

b Yos 3:13
Yos 3:16

c Kum 4:9

d Yos 4:2
Mdo 26:7

e Kum 27:2
Yos 4:3
Yos 4:19

f Yos 3:17

g Yos 3:13

h Kum 27:2
Kum 34:9

i Zb 119:60

j Yos 3:8
Yos 3:17

k Yos 1:12

l Kut 13:18
Hes 32:27
Yos 1:14

Safu ya 2

a Hes 32:21
Hes 32:29

b Yos 3:7
Zb 75:7

c Kut 14:31

d Kut 25:22

e Hes 4:15

f Yos 3:13

g Yos 3:15

h Yos 4:3
Yos 5:9
Yos 10:6
Mik 6:5

i Kum 27:2
Yos 4:8

j Yos 4:6
Zb 44:1

k Yos 3:17
Zb 66:6

23 Yehova Mungu wenu alipoyakausha maji ya Yordani mbele yao mpaka walipokwisha kuvuka, kama vile Yehova Mungu wenu alivyokuwa ameifanya Bahari Nyekundu alipoikausha mbele yetu mpaka tulipokwisha kuvuka;[a] **24** ili watu wote wa dunia wapate kuujua mkono wa Yehova,[b] kwamba ni wenye nguvu;[c] ili mpate kumwogopa Yehova Mungu wenu sikuzote.'"[d]

5 Na ikawa kwamba, mara tu wafalme wote wa Waamori,[e] waliokuwa ng'ambo ya Yordani upande wa magharibi, na wafalme wote wa Wakanaani,[f] waliokuwa kando ya bahari, waliposikia kwamba Yehova alikuwa amekausha maji ya Yordani mbele ya wana wa Israeli mpaka walipokuwa wamevuka, ndipo mioyo yao ikaanza kuyeyuka,[g] wala haikuwamo roho yoyote ya nguvu iliyobaki ndani yao tena kwa sababu ya wana wa Israeli.[h]

2 Na wakati huo Yehova akamwambia Yoshua: "Jitengenezee visu vya jiwe gumu, uwatahiri[i] tena wana wa Israeli mara ya pili." **3** Basi Yoshua akajitengenezea visu vya jiwe gumu, akawatahiri wana wa Israeli katika Gibeath-haaralothi.[j] **4** Na hii ndiyo sababu iliyomfanya Yoshua awatahiri: watu wote waliotoka Misri, waume, wanaume wote wa vita, walikuwa wamekufa[k] njiani katika nyika walipokuwa wakitoka Misri. **5** Kwa maana watu wote waliotoka walikuwa wametahiriwa, lakini watu wote waliozaliwa katika nyika njiani walipokuwa wakitoka Misri hawakuwa wamewatahiri. **6** Kwa maana wana wa Israeli walikuwa wametembea miaka 40[l] nyikani, mpaka lilipokwisha taifa lote la wale wanaume wa vita waliotoka Misri ambao hawakuisikiliza sauti ya Yehova, ambao Yehova alikuwa amewaapia kwamba hatawaruhusu kamwe waione nchi[a] ambayo Yehova alikuwa amewaapia mababu zao kwamba atatupa sisi,[b] nchi inayotiririka maziwa na asali.[c] **7** Naye akawasimamisha wana wao badala yao.[d] Yoshua akawatahiri hao wana, kwa sababu walikuwa hawajatahiriwa, kwa maana hawakuwa wamewatahiri njiani.

8 Kisha ikawa kwamba walipokuwa wamemaliza kutahiri taifa lote, wakaendelea kukaa mahali pao kambini mpaka walipopona.[e]

9 Ndipo Yehova akamwambia Yoshua: "Leo nimeondolea mbali aibu ya Misri itoke juu yenu."[f] Basi jina la mahali hapo likaitwa Gilgali[g] mpaka leo hii.

10 Na wana wa Israeli wakaendelea kupiga kambi katika Gilgali, nao wakasherehekea pasaka siku ya kumi na nne ya mwezi huo,[h] wakati wa jioni, katika nchi tambarare za jangwa la Yeriko. **11** Nao wakaanza kula mazao ya nchi siku iliyofuata pasaka, keki zisizo na chachu[i] na nafaka zilizochomwa, siku ileile. **12** Ndipo mana ikaacha kuanguka siku iliyofuata walipokuwa wamekula mazao ya nchi, wala mana haikuja tena kwa ajili ya wana wa Israeli,[j] nao wakaanza kula mazao ya nchi ya Kanaani mwaka huo.[k]

13 Kisha ikawa kwamba Yoshua alipokuwa karibu na Yeriko, akainua macho yake na kuangalia, na tazama, palikuwa na mwanamume[l] aliyesimama mbele yake akiwa na upanga

SURA 4
a Kut 14:21; Ne 9:11; Zb 78:13; Isa 43:16; Isa 63:12; Ebr 11:29
b Kut 9:16; Kum 28:10; 1Sa 17:46; 1Fa 8:42; 2Fa 5:15; 2Fa 19:19
c Kut 15:6; Zb 89:13; Zb 106:8
d Kum 6:2; Zb 76:7; Yer 10:7; 1Pe 2:17

SURA 5
e Mwa 10:16
f Mwa 12:6; Hes 13:29; Amu 3:3
g Kut 15:15; Yos 2:9; Yos 2:11
h Yos 2:24
i Mwa 17:11; Kut 4:25
j Yos 5:9
k Hes 14:29; Hes 26:65; Kum 2:14; 1Ko 10:5; Ebr 3:17
l Hes 14:33; Kum 1:3; Zb 95:10

Safu ya 2
a Hes 14:23; Kum 1:35; Zb 106:26
b Mwa 13:15; Kut 33:1; Mdo 7:5
c Kut 3:8; Hes 13:27; Kum 27:3; Eze 20:6
d Hes 14:31; Kum 1:39
e Mwa 34:25
f Mwa 34:14; Zb 119:39; Yer 9:25; Yer 9:26
g Yos 4:19; Yos 5:3
h Kut 12:24; Hes 9:5
i Kut 12:18; Kut 13:6; Law 23:6
j Kut 16:35
k Kum 6:11; Kum 8:10
l Mwa 18:2; Kut 23:23; Amu 13:6; Mdo 1:10

uliochomolewa mkononi mwake.[a] Kwa hiyo Yoshua akamwendea na kumwambia: "Je, wewe uko upande wetu au upande wa adui zetu?" **14** Ndipo yeye akasema: "Hapana, lakini mimi—nikiwa mkuu wa jeshi la Yehova nimekuja sasa."[b] Basi Yoshua akaanguka kifudifudi,[c] akasujudu na kumwambia: "Bwana wangu anamwambia nini mtumishi wake?" **15** Ndipo mkuu wa jeshi la Yehova akamwambia Yoshua: "Vua viatu vyako kutoka miguuni mwako, kwa sababu mahali ambapo umesimama ni patakatifu." Yoshua akavua mara moja.[d]

6 Basi jiji la Yeriko lilikuwa limefungwa imara kwa sababu ya wana wa Israeli, hakuna mtu aliyetoka nje wala kuingia ndani.[e]

2 Na Yehova akamwambia Yoshua: "Tazama, nimetia mkononi mwako Yeriko na mfalme wake, na mashujaa, wanaume wenye nguvu.[f] **3** Nanyi nyote wanaume wa vita mtapiga mwendo kulizunguka jiji, mkilizunguka jiji mara moja. Hivyo ndivyo utakavyofanya kwa siku sita. **4** Na makuhani saba wachukue pembe saba za kondoo-dume, mbele ya hilo Sanduku, na siku ya saba mpige mwendo kuzunguka jiji mara saba, nao makuhani wazipige pembe.[g] **5** Na itatukia kwamba watakapopiga pembe ya kondoo-dume, mtakapoisikia sauti ya pembe, watu wote watapaaza kelele kubwa za vita;[h] na ukuta wa jiji utaanguka chini,[i] kisha watu watapanda, kila mmoja akisonga mbele moja kwa moja."

6 Basi Yoshua mwana wa Nuni akawaita makuhani[j] na kuwaambia: "Lichukueni sanduku la agano,[a] na makuhani saba wachukue pembe saba za kondoo-dume mbele ya sanduku[b] la Yehova." **7** Naye akaendelea kuwaambia watu: "Piteni, mpige mwendo kulizunguka jiji, na kikosi kilichotayarishwa kwa ajili ya vita[c] kipite mbele ya sanduku la Yehova." **8** Basi ikawa kama vile Yoshua alivyowaambia watu; na makuhani saba waliochukua pembe saba za kondoo-dume mbele za Yehova wakapita na kuzipiga pembe hizo, nalo sanduku la agano la Yehova lilikuwa likiwafuata. **9** Na kile kikosi kilichotayarishwa kwa ajili ya vita kilikuwa kinaenda mbele ya makuhani waliokuwa wakizipiga pembe, na wakati huohuo kikosi cha nyuma[d] kilikuwa kikilifuata Sanduku nazo zile pembe zilikuwa zikipigwa kwa mfululizo.

10 Basi Yoshua alikuwa amewaamuru watu,[e] akisema: "Msipaaze sauti wala kuacha sauti zenu zisikike, na neno lolote lisitoke katika vinywa vyenu mpaka siku nitakapowaambia, 'Paazeni sauti!' Ndipo mtakapopaaza sauti."[f] **11** Naye akalipeleka sanduku la agano la Yehova lizunguke jiji, likazunguka mara moja, kisha wakaenda kambini na kukaa usiku kucha katika kambi.

12 Ndipo Yoshua akaamka asubuhi na mapema,[g] nao makuhani wakalichukua sanduku[h] la Yehova, **13** na makuhani saba waliochukua pembe saba za kondoo-dume mbele ya sanduku la Yehova walikuwa wanatembea, wakizipiga pembe kwa mfululizo, na kile kikosi kilichotayarishwa kwa ajili ya vita kilikuwa kinatembea mbele yao, huku kile kikosi

SURA 5
a Hes 22:23; 1Nya 21:16
b Kut 23:20; 1Fa 22:19; Zb 103:20; Zb 148:2; Da 10:13
c Mwa 17:3
d Kut 3:5

SURA 6
e Yos 2:9
f Hes 14:9; Kum 7:24; Amu 11:24; Ne 9:24
g Amu 3:27; Amu 7:22; 2Sa 2:28; Sef 1:16
h Yer 50:15; Ho 5:8
i Ebr 11:30
j Kum 20:2

Safu ya 2
a Kum 31:25
b Hes 4:15
c Hes 10:14; Hes 10:18; Hes 10:22; Yos 1:14; Yos 4:13
d Hes 10:25
e Kum 34:9
f Yos 1:18
g Yos 3:1
h Hes 3:31; Hes 4:15; Kum 31:9; 1Nya 15:2

cha nyuma kikifuata sanduku
la Yehova nazo pembe zilikuwa
zikipigwa kwa mfululizo.[a]
14 Nao wakalizunguka jiji siku
ya pili mara moja, kisha waka-
rudi kambini. Hivyo ndivyo wa-
livyofanya kwa siku sita.[b]
15 Kisha, katika siku ya saba
wakaamka mapema, mara ku-
lipopambazuka, nao wakalizu-
nguka jiji vivyo hivyo mara saba.
Siku hiyo peke yake walizungu-
ka jiji mara saba.[c] **16** Na ikawa
kwamba mara ya saba makuha-
ni walipiga pembe, ndipo Yoshua
akawaambia watu: "Paazeni sau-
ti;[d] kwa maana Yehova amewapa
ninyi jiji hili.[e] **17** Na jiji hili li-
takuwa kitu cha kuharibiwa;[f]
jiji lenyewe pamoja na kila kitu
kilicho ndani yake ni vya Yeho-
va. Rahabu[g] yule kahaba peke
yake ndiye atakayeendelea kui-
shi, yeye na wote walio pamoja
naye katika nyumba, kwa kuwa
aliwaficha wajumbe tuliowatu-
ma.[h] **18** Nanyi mjiepushe tu
na kitu kilichotengwa kwa aji-
li ya kuharibiwa,[i] msije mkawa
na tamaa[j] na kuchukua sehemu
ya vitu vilivyotengwa kwa aji-
li ya kuharibiwa[k] na kuifanya
kambi ya Israeli kuwa kitu ki-
lichotengwa kwa ajili ya ku-
haribiwa na kuileteа laana.[l]
19 Lakini fedha yote na dhaha-
bu na vyombo vya shaba na chu-
ma ni vitu vitakatifu kwa Yeho-
va.[m] Viwekwe katika hazina ya
Yehova."[n]
20 Ndipo watu wakapaaza
sauti, walipopiga pembe.[o] Kisha
ikawa kwamba mara tu watu
walipoisikia sauti ya pembe
na watu wakapaaza kelele ku-
bwa za vita, ndipo ukuta ukaa-
nza kuanguka chini kabisa.[p] Ki-
sha watu wakapanda juu, waka-
ingia katika jiji, kila mmoja aka-
songa mbele moja kwa moja, na
kuliteka jiji. **21** Wakaangami-
za kila kitu kilichokuwa ndani
ya jiji hilo, kuanzia mwanamu-
me mpaka mwanamke, kuanzia
kijana mpaka mzee hata ng'o-
mbe na kondoo na punda, kwa
makali ya upanga.[a]
22 Na Yoshua akawaambia
wale wanaume wawili waliokuwa
wameipeleleza nchi: "Ingie-
ni katika nyumba ya yule mwa-
namke, yule kahaba, mkamtoe
nje mwanamke huyo na wote
walio wake, kama vile mlivyo-
mwapia."[b] **23** Basi wale vija-
na waliokuwa wamefanya upe-
lelezi wakaingia, wakamtoa nje
Rahabu na baba yake na mama
yake na ndugu zake na wote wa-
liokuwa wake, ndiyo, wakawa-
toa nje jamaa zake wote;[c] nao
wakawaweka nje ya kambi ya
Israeli.
24 Kisha wakaliteketeza jiji
kwa moto na kila kitu kilicho-
kuwamo.[d] Isipokuwa fedha na
dhahabu na vyombo vya sha-
ba na chuma wakaviweka kati-
ka hazina ya nyumba ya Yeho-
va.[e] **25** Naye Yoshua akawahi-
fadhi hai Rahabu yule kaha-
ba na nyumba ya baba yake
na wote waliokuwa wake;[f] naye
anakaa katikati ya Israeli mpa-
ka leo hii,[g] kwa sababu aliwafi-
cha wajumbe ambao Yoshua ali-
watuma kupeleleza Yeriko.[h]
26 Ndipo Yoshua akatanga-
za kiapo wakati huo, akasema:
"Na alaaniwe mbele za Yeho-
va mtu yule atakayesimama na
kujenga jiji hili, yaani, Yeriko.
Kwa kufiwa na mzaliwa wake
wa kwanza na auweke msingi
wake, na kwa kufiwa na mwana
wake aliye mdogo zaidi na aisi-
mamishe milango yake."[i]
27 Basi Yehova akawa pamo-
ja na Yoshua,[j] na sifa yake ikae-
nea katika dunia yote.[k]

SURA 6
a Yos 6:4
b Yos 6:3
c Yos 6:4
d Yos 6:5
Yos 6:10
2Nya 13:15
e Kum 9:1
Yos 6:1
f Law 27:28
Hes 21:3
Kum 7:2
Kum 20:16
g Yos 2:1
Mt 1:5
Ebr 11:31
h Mwa 12:3
Yos 2:4
Yos 2:6
Mt 25:40
Ebr 6:10
Yak 2:25
i Kum 7:26
j Kum 13:17
Yos 7:21
Ebr 13:5
k Yos 7:11
l Yos 7:25
1Nya 2:7
m Hes 31:22
n Yos 6:24
2Sa 8:11
1Fa 7:51
1Nya 18:11
o Yos 6:4
Yos 6:16
p Yos 6:5
Ebr 11:30

Safu ya 2
a Law 27:29
Kum 7:2
Kum 20:16
1Sa 15:3
b Yos 2:14
Ebr 11:31
c Yos 2:13
Yos 2:18
d Kum 13:16
e Yos 6:19
f Yos 2:14
Yos 6:17
Yos 6:22
g Mt 1:5
h Ebr 6:10
Yak 2:25
i 1Fa 16:34
j Kum 31:6
Yos 1:5
Ro 8:31
k Yos 9:1
Yos 9:9

7 Kisha wana wa Israeli wakafanya tendo la kukosa uaminifu kuhusiana na kitu kilichotengwa kwa ajili ya kuharibiwa kwa kuwa Akani[a] mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila la Yuda, alichukua sehemu ya vitu vilivyotengwa kwa ajili ya kuharibiwa.[b] Ndipo hasira ya Yehova ikawaka juu ya wana wa Israeli.[c]

2 Basi Yoshua akatuma wanaume kutoka Yeriko kwenda Ai,[d] jiji lililo karibu na Bethaveni,[e] upande wa mashariki wa Betheli,[f] na kuwaambia: "Pandeni juu, mkaipeleleze nchi." Basi wanaume hao wakapanda, wakapeleleza Ai.[g] **3** Kisha wakarudi kwa Yoshua wakamwambia: "Usiache watu wote waende. Acha wanaume elfu mbili hivi au wanaume elfu tatu hivi waende kupiga Ai. Usiwachoshe watu wote kwa kuwapeleka huko, kwa maana watu hao ni wachache."

4 Basi karibu wanaume elfu tatu kati ya watu wakaenda huko, lakini wakakimbia mbele ya wanaume wa Ai.[h] **5** Na wanaume wa Ai wakawapiga na kuwaua karibu watu 36 kati yao, wakawafuatilia[i] kutoka mbele ya lango mpaka Shebarimu, wakaendelea kuwapiga na kuwaua kwenye mteremko. Basi mioyo ya watu ikaanza kuyeyuka, ikawa kama maji.[j]

6 Ndipo Yoshua akararua nguo zake za kujitanda, akaanguka kifudifudi[k] mbele ya sanduku la Yehova mpaka jioni, yeye na wanaume wazee wa Israeli, nao wakawa wakitia mavumbi vichwani mwao.[l] **7** Kisha Yoshua akasema: "Ole wangu, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, kwa nini uliwaleta watu hawa njia yote hiyo kuuvuka Yordani, ili tu kututia mkononi mwa Waamori, watuangamize? Laiti tungejichagulia wenyewe tuendelee kukaa ng'ambo ile nyingine ya Yordani![a] **8** Nakuomba radhi, Ee Yehova, lakini niseme nini baada ya Israeli kugeuza mgongo wake mbele ya adui zake? **9** Nao Wakanaani na wakaaji wote wa nchi hii watasikia habari hizi, nao hakika watatuzunguka na kulikatilia mbali jina letu kutoka duniani;[b] nawe utafanya nini kwa ajili ya jina lako kuu?"[c]

10 Naye Yehova akamwambia Yoshua: "Simama, wewe! Kwa nini unaanguka kifudifudi? **11** Israeli wametenda dhambi, nao wamevunja agano langu[d] ambalo niliwaamuru; tena wamechukua sehemu ya vitu vilivyotengwa kwa ajili ya kuharibiwa,[e] tena wameiba,[f] tena wamevificha[g] na kuvitia katikati ya vyombo vyao wenyewe.[h] **12** Na wana wa Israeli hawataweza kusimama juu ya adui zao.[i] Watawageuzia mgongo adui zao, kwa sababu wamekuwa kitu kilichotengwa kwa ajili ya kuharibiwa. Sitakuwa pamoja nanyi tena isipokuwa mharibu kutoka katikati yenu kitu kilichotengwa kwa ajili ya kuharibiwa.[j] **13** Simama! Watakase watu,[k] nawe useme, 'Jitakaseni kesho, kwa maana Yehova Mungu wa Israeli amesema hivi: "Kitu kilichotengwa kwa ajili ya kuharibiwa kimo katikati yenu, Ee Israeli.[l] Hamtaweza kusimama juu ya adui zenu mpaka mtakapoondoa katikati yenu kile kitu kilichotengwa kwa ajili ya kuharibiwa. **14** Nanyi mtakuja asubuhi, kabila kwa kabila, na

SURA 7
a Yos 22:20
1Nya 2:7
b Kum 7:26
Yos 6:17
c Yos 6:18
d Mwa 12:8
Yos 12:9
e Yos 18:12
f Mwa 28:19
g Yos 2:1
h Law 26:17
Kum 28:25
Kum 32:30
Isa 30:17
Isa 59:2
i Kum 28:45
j Law 26:36
Isa 13:7
k Hes 16:22
Hes 20:6
l Ne 9:1
Ayu 2:12

Safu ya 2
a Yos 3:1
b Zb 83:4
c Kut 32:12
Kum 32:27
Zb 106:8
Zb 143:11
Eze 20:9
d Kut 24:7
1Sa 2:25
e Yos 6:17
f Kut 20:15
Isa 61:8
Mt 15:19
g Yer 32:19
Ebr 4:13
h Yos 7:21
i Amu 2:14
j Kum 7:26
Yos 6:18
k Kut 19:10
l Yos 6:18

itatukia kwamba kabila ambalo Yehova atalichagua[a] litakaribia, familia kwa familia, na familia ambayo Yehova ataichagua itakaribia, nyumba kwa nyumba, na nyumba ambayo Yehova ataichagua itakaribia, mwanamume kwa mwanamume. **15** Na itatukia kwamba mtu atakayechaguliwa akiwa na kile kitu kilichotengwa kwa ajili ya kuharibiwa atateketezwa kwa moto,[b] yeye na vyote vilivyo vyake, kwa sababu amevunja agano[c] la Yehova na kwa sababu amefanya upumbavu wenye kufedhehesha katika Israeli.”’”[d]

16 Ndipo Yoshua akaamka asubuhi na mapema, akawaleta Israeli karibu, kabila kwa kabila, na kabila la Yuda likachaguliwa. **17** Kisha akaleta karibu familia za Yuda, naye akachagua familia ya Wazera,[e] kisha akaleta karibu familia ya Wazera, mwanamume kwa mwanamume, na Zabdi akachaguliwa. **18** Mwishowe akaleta karibu nyumba yake, mwanamume kwa mwanamume, na Akani mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila la Yuda, akachaguliwa.[f] **19** Ndipo Yoshua akamwambia Akani: “Tafadhali, mwanangu, mpe Yehova Mungu wa Israeli utukufu[g] na uungame kwake,[h] tafadhali niambie,[i] Umefanya nini? Usinifiche[j] jambo hili.”

20 Ndipo Akani akamjibu Yoshua na kusema: “Ni kweli—nimemtendea dhambi Yehova Mungu wa Israeli,[k] nami nimefanya hivi na hivi. **21** Nilipoona[l] katikati ya nyara vazi rasmi kutoka Shinari,[m] lenye kupendeza, na shekeli 200 za fedha na kipande kimoja cha dhahabu, uzito wake ukiwa shekeli 50, ndipo nikavitamani[a] vitu hivyo, halafu nikavichukua;[b] na, tazama! vimefichwa chini ya udongo katikati ya hema langu na zile pesa chini yake.”[c]

22 Mara moja Yoshua akatuma wajumbe, wakakimbia kwenda hemani, na, tazama! vile vitu vilikuwa vimefichwa katika hema lake, na zile pesa chini yake. **23** Basi wakavichukua kutoka katikati ya lile hema, wakavileta kwa Yoshua na kwa wana wote wa Israeli na kuvimwaga mbele za Yehova. **24** Basi Yoshua, na Israeli wote pamoja naye, wakamchukua Akani[d] mwana wa Zera na ile fedha na lile vazi rasmi na kile kipande cha dhahabu[e] na wanawe na binti zake na ng’ombe zake na punda zake na kundi lake na hema lake na kila kitu kilichokuwa chake, wakawaleta katika nchi tambarare ya chini ya Akori.[f] **25** Ndipo Yoshua akasema: “Kwa nini umeleta laana juu yetu?[g] Leo hii Yehova ataleta laana juu yako.” Ndipo Israeli wote wakampiga kwa mawe,[h] kisha wakawateketeza kwa moto.[i] Kwa hiyo wakawapiga kwa mawe. **26** Nao wakaweka rundo kubwa la mawe juu yake, mpaka leo hii.[j] Ndipo Yehova akaiacha hasira yake inayowaka.[k] Ndiyo sababu jina la mahali hapo limeitwa Nchi Tambarare ya Chini ya Akori,[l] mpaka leo hii.

8 Kisha Yehova akamwambia Yoshua: “Usiogope wala usiwe na hofu.[m] Wachukue pamoja nawe watu wote wa vita kisha usimame, mwende Ai. Tazama, nimemtia mkononi mwako mfalme wa Ai na watu wake na jiji lake na nchi yake.[n] **2** Nawe unapaswa kulitendea Ai na mfalme wake kama

SURA 7

a Met 16:33
b Yos 1:18
Yos 7:25
c Kut 24:7
Yos 7:11
Amu 2:20
d Amu 20:6
2Sa 13:12
e Mwa 38:30
Hes 26:20
1Nya 2:4
f 1Sa 14:42
Met 13:21
Met 16:33
Yer 2:26
Yon 1:7
Mdo 5:3
g 2Nya 19:6
Yer 13:16
h Zb 32:5
Zb 51:4
1Ti 5:24
i 1Sa 14:43
Met 28:13
j Ayu 31:33
k 1Sa 2:25
l 1Yo 2:16
m Mwa 10:10

Safu ya 2

a Kut 20:17
Lu 12:15
2Pe 2:14
b Mik 2:2
Yak 1:15
c Zb 10:11
Isa 29:15
d Yos 7:1
Yos 22:20
e Yos 6:19
f Yos 15:7
Isa 65:10
Ho 2:15
g Yos 6:18
1Nya 2:7
h Law 24:14
Yos 1:18
i Mwa 38:24
Law 20:14
Law 21:9
Yos 7:15
j Yos 8:29
Yos 10:27
2Sa 18:17
k Kum 13:17
l Yos 15:7
Isa 65:10
Ho 2:15

SURA 8

m Kum 1:21
Kum 7:18
Kum 31:8
Yos 1:9
Zb 27:1
Isa 12:2
Ro 8:31
n Yos 2:24
Zb 44:3
Mdo 7:45

vile ulivyolitendea Yeriko na
mfalme wake.[a] Lakini mnawe-
za kupora nyara zake na wanya-
ma wake wa kufugwa kwa ajili
yenu wenyewe.[b] Weka kikundi
cha kulivizia jiji upande wake
wa nyuma."[c]
3 Basi Yoshua na watu wote
wa vita[d] wakasimama waende
Ai, kisha Yoshua akachagua wa-
naume wenye nguvu[e] 30,000,
akawatuma wakati wa usiku.
4 Naye akawaamuru, akisema:
"Angalieni, mtajificha na kuliviziaf jiji, upande wa nyuma wa jiji.
Msiende mbali sana na jiji, na-
nyi nyote kaeni tayari. **5** La-
kini mimi na watu wote walio
pamoja nami, tutaenda karibu
na jiji. Na itatukia kwamba, wa-
kitoka nje kukutana nasi kama
walivyofanya pale mwanzoni,[g]
ndipo sisi tutakapokimbia mbe-
le yao. **6** Nao watatoka nje
watufuate mpaka tutakapoku-
wa tumewavuta mbali na jiji
hilo, kwa maana watasema, 'Wa-
nakimbia mbele yetu kama wali-
vyofanya pale mwanzoni.'[h] Nasi
tutakimbia mbele yao. **7** Ki-
sha ninyi mtasimama kutoka
hapo mlipovizia, nanyi mta-
likamata jiji; na Yehova Mungu
wenu hakika atalitia jiji hilo mi-
kononi mwenu.[i] **8** Na itatukia
kwamba mara tu mtakapoku-
wa mmelikamata jiji, mtalite-
keteza jiji kwa moto.[j] Mnapa-
swa kufanya kulingana na neno
la Yehova. Angalieni, nimewaa-
muru ninyi."[k]
9 Kisha Yoshua akawatuma,
nao wakaenda mahali pa kuvi-
zia, wakapiga kambi kati ya Be-
theli na Ai upande wa magharibi wa Ai, naye Yoshua akaende-
lea kukaa usiku huo katikati ya
watu.
10 Ndipo Yoshua akaamka
asubuhi na mapema,[l] akawaka-
gua watu, kisha akapanda kwe-
nda Ai mbele ya watu, yeye pa-
moja na wanaume wazee wa
Israeli. **11** Na watu wote wa
vita[a] waliokuwa pamoja naye
wakaenda, wapate kukaribia na
kuwa mbele ya jiji, nao wakaa-
nza kupiga kambi upande wa ka-
skazini wa Ai, pakiwa na bonde
kati yao na Ai. **12** Wakati hu-
ohuo akachukua wanaume elfu
tano hivi, akawaweka kuvizia[b]
kati ya Betheli[c] na Ai, upande
wa magharibi wa jiji. **13** Basi
watu wakaweka kambi kuu ili-
yokuwa upande wa kaskazini wa
jiji[d] na wale wa nyuma kabisa
waliokuwa upande wa magharibi wa jiji,[e] kisha Yoshua akaanza
kwenda usiku huo katikati ya ile
nchi tambarare ya chini.
14 Na ikawa kwamba, mara
tu mfalme wa Ai alipoona hilo,
wanaume wa jiji lile wakafa-
nya haraka, wakaamka mape-
ma, wakatoka nje wakutane ku-
pigana na Israeli, yeye na watu
wake wote, kwa wakati uliowe-
kwa, mbele ya ile nchi tambar-
are ya jangwa. Lakini yeye
hakujua kwamba palikuwa na
waliomvizia upande wa nyuma
wa jiji.[f] **15** Wakati Yoshua na
Israeli wote walipopigwa mbe-
le yao,[g] wakaanza kukimbia ku-
pitia njia ya nyika.[h] **16** Ndipo
watu wote waliokuwa ndani ya
jiji wakaitwa wawafuatilie, nao
wakamfuatilia Yoshua na ku-
vutwa mbali na jiji.[i] **17** Haku-
baki mtu yeyote ndani ya Ai
na Betheli ambaye hakufuatilia
Israeli, hivyo wakaliacha jiji
wazi kabisa, wakawafuatilia
Israeli.
18 Sasa Yehova akamwa-
mbia Yoshua: "Nyoosha mkuki
ulio mkononi mwako kuelekea
Ai,[j] kwa maana nitalitia mkono-
ni mwako."[k] Basi Yoshua akau-

SURA 8
a Yos 6:21
b Ayu 27:17
Met 13:22
Mhu 2:26
c Met 20:18
d Yos 8:11
e Kum 3:18
Kum 20:8
Ebr 11:34
f Amu 20:29
2Nya 13:13
g Yos 7:5
h Kut 15:9
Yos 8:16
i Yos 2:24
Met 21:31
j Yos 8:19
Yos 8:28
k Yos 1:9
Yos 1:16
l Yos 3:1
Yos 6:12

Safu ya 2
a Yos 8:1
Yos 8:3
b Yos 8:2
Amu 20:29
c Mwa 28:19
d Yos 8:5
e Yos 8:4
f Amu 20:34
Met 14:15
g Amu 20:36
h Yos 8:6
Yos 16:1
Yos 18:12
i Kut 15:9
Amu 20:31
Zb 9:16
j Kut 17:11
Yos 8:7
Yos 8:26
k Kum 7:24
Yos 1:5

nyoosha mkuki uliokuwa mkononi mwake kuelekea jiji lile.
19 Na waliovizia wakasimama haraka kutoka mahali pao, nao wakaanza kukimbia mara tu aliponyoosha mkono wake, wakaingia ndani ya jiji na kulikamata.[a] Kisha wakafanya haraka na kuliwasha moto jiji hilo.[b]

20 Ndipo watu wa Ai wakaanza kugeuka nyuma wakaona, na tazama, moshi wa jiji hilo ulikuwa unapaa juu mbinguni, na ndani yao haukubaki uwezo wowote wa kukimbia huku au huku. Kisha wale watu waliokuwa wakikimbilia nyikani wakawageukia wale waliokuwa wakiwafuatilia. **21** Na Yoshua na Israeli wote wakaona kwamba waliovizia[c] walikuwa wamelikamata jiji hilo, na kwamba moshi wa jiji ulikuwa unapaa juu, kwa hiyo wakageuka, wakaanza kuwapiga na kuwaua watu wa Ai. **22** Na hao wengine wakatoka katika jiji kuja kukutana nao, hata wale wakawa katikati ya Israeli, hawa upande huu na hawa upande ule, nao wakawaua hata asibaki yeyote kati yao, mwenye kuokoka wala mwenye kupona.[d] **23** Naye mfalme[e] wa Ai wakamkamata akiwa hai, wakamleta karibu na Yoshua.

24 Na ikawa kwamba Israeli walipokuwa wakimaliza kuwaua wakaaji wote wa Ai uwanjani, katika nyika ambamo walikuwa wamewafuatilia, wote waliendelea kuanguka, kwa makali ya upanga mpaka walipokwisha. Kisha Israeli wote wakarudi Ai na kulipiga kwa makali ya upanga. **25** Na wote walioanguka siku hiyo, kuanzia mwanamume mpaka mwanamke, jumla yao ilikuwa kumi na mbili elfu, watu wote wa Ai. **26** Yoshua naye hakuurudisha nyuma mkono wake ambao alitumia kunyoosha ule mkuki[a] mpaka alipokuwa amewaangamiza[b] wakaaji wote wa Ai. **27** Ni wanyama wa kufugwa peke yao na nyara za jiji ndizo ambazo Israeli waliteka kwa ajili yao wenyewe, kulingana na neno la Yehova ambalo alikuwa amemwamuru Yoshua.[c]

28 Kisha Yoshua akateketeza Ai na kulifanya kuwa kilima kinachodumu mpaka wakati usio na kipimo,[d] na kuwa ukiwa mpaka leo hii. **29** Naye akamtundika mfalme wa Ai[e] juu ya mti mpaka jioni;[f] na jua lilipokaribia kutua, Yoshua akatoa amri nao wakachukua maiti yake[g] kutoka mtini na kuitupa kwenye mwingilio wa lango la jiji nao wakaweka rundo kubwa la mawe juu yake, mpaka leo hii.

30 Ndipo Yoshua akaanza kujenga madhabahu[h] kwa Yehova Mungu wa Israeli, katika Mlima Ebali,[i] **31** kama vile Musa mtumishi wa Yehova alivyokuwa amewaamuru wana wa Israeli, kama ilivyoandikwa katika kitabu cha sheria[j] ya Musa: "Madhabahu ya mawe mazima, ambayo chombo cha chuma hakikutumiwa juu yake";[k] nao wakatoa juu yake matoleo ya kuteketezwa kwa Yehova na kutoa dhabihu za ushirika.[l]

32 Kisha akaandika hapo juu ya mawe nakala[m] ya maandishi ya sheria ya Musa ambayo alikuwa ameandika mbele ya wana wa Israeli.[n] **33** Na Israeli wote na wanaume wao wazee[o] na maofisa na waamuzi wao walikuwa wamesimama upande huu wa Sanduku na upande ule mwingine mbele ya makuhani[p] Walawi, waliochukua sanduku la

SURA 8

a Yos 8:7
b Yos 8:8
Yos 8:28
c Yos 8:2
Amu 20:29
d Law 27:29
Kum 7:2
e Yos 8:29
Yos 12:9

Safu ya 2

a Kut 17:11
Yos 8:18
b Law 27:29
c Hes 31:26
Yos 8:2
Ayu 27:17
Met 13:22
Mhu 2:26
d Yos 8:8
e Yos 12:9
f Kum 21:22
g Kum 21:23
Yos 10:27
h Kut 20:24
i Kum 11:29
Kum 27:5
j Kum 31:9
Yos 1:8
2Nya 34:14
Da 9:13
Mal 4:4
k Kut 20:25
Kum 27:6
l Kut 20:24
Kum 27:7
m Kum 27:3
Kum 27:8
2Ko 3:3
n Kut 24:4
Kut 34:27
o Kum 29:10
p Kum 31:9

agano la Yehova,[a] mkaaji mgeni
na mwenyeji[b] vilevile, nusu yao
walisimama mbele ya Mlima Ge-
rizimu[c] na nusu ile nyingine
mbele ya Mlima Ebali,[d] (kama
vile Musa mtumishi wa Yehova
alivyokuwa ameamuru,)[e] ili ku-
wabariki[f] watu wa Israeli kwa-
nza. **34** Kisha akasoma kwa
sauti maneno yote ya sheria,[g]
baraka[h] na laana,[i] kulingana na
yote ambayo yameandikwa ka-
tika kitabu cha sheria. **35** Ha-
kuna neno lolote kati ya yote
ambayo Musa alikuwa amea-
muru ambalo Yoshua hakuso-
ma kwa sauti mbele ya kutani-
ko lote la Israeli,[j] pamoja na wa-
nawake[k] na watoto wadogo[l] na
wakaaji wageni[m] waliokuwa ka-
tikati yao.

9 Na ikawa kwamba mara tu
wafalme wote[n] waliokuwa
ng'ambo ya Yordani iliyo kati-
ka eneo lenye milima na katika
Shefela na kando ya pwani yote
ya ile Bahari Kuu[o] na mbele ya
Lebanoni,[p] Wahiti[q] na Waamori,
Wakanaani,[r] Waperizi,[s] Wahivi
na Wayebusi,[t] waliposikia haba-
ri hizo, **2** wakaanza kukusa-
nyika pamoja ili kupigana vita
na Yoshua na Israeli kwa kauli
moja.[u]

3 Na wakaaji wa Gibeoni[v]
wakasikia mambo ambayo Yo-
shua alikuwa ametendea Yeri-
ko[w] na Ai.[x] **4** Basi wao, kwa
kupenda kwao wenyewe, waka-
tenda kwa werevu,[y] wakajiwe-
kea akiba ya vyakula na kuchu-
kua magunia yaliyochakaa kwa
ajili ya punda zao, na viriba vya
divai vilivyochakaa, vilivyopa-
suka na kufungwa,[z] **5** na via-
tu vilivyochakaa na kupigwa
viraka miguuni mwao, waka-
vaa mavazi yaliyochakaa, na
mkate wote wa vyakula vyao
ukawa mkavu na wenye kuvu-

SURA 8

a Kum 31:25
b Law 24:22
Hes 15:16
c Kum 27:12
d Kum 27:13
e Kum 11:29
f Met 10:6
g Kum 31:9
Ne 8:3
h Law 26:3
Kum 28:2
i Kum 27:15
Kum 28:15
Kum 29:21
j Kum 4:2
Kum 12:32
k Kum 31:12
Ne 8:2
l Kum 29:11
m Law 24:22
Hes 15:16

SURA 9

n Yos 12:7
o Hes 34:6
p Kum 1:7
q Mwa 15:20
r Kut 3:17
Kut 23:23
s Kum 7:1
t Kut 13:5
u Yos 24:11
Zb 83:4
Zb 83:5
v Yos 10:2
Yos 11:19
w Yos 6:20
x Yos 8:24
y Met 14:15
Met 22:3
z Mt 9:17

Safu ya 2

a Yos 5:10
Yos 10:43
b Lu 14:32
c Mwa 10:17
Mwa 34:2
Kut 3:8
d Kut 23:32
Kut 34:12
Kum 7:2
Kum 20:16
Kum 20:18
Amu 2:2
e 2Fa 10:5
f Kum 20:15
g 1Fa 8:41
2Nya 6:32
Met 18:10
h Kut 9:16
Kut 15:14
Yos 2:10
i Hes 21:21
Hes 21:24
Kum 2:34
j Hes 21:33
Hes 21:35
Kum 3:3
k Kum 1:4
Yos 12:4
l Ayu 12:12
Ayu 32:7
m Kum 20:11
n Yos 9:6
o Yos 9:5
p Yos 9:4
Mk 2:22

njika-vunjika. **6** Kisha waka-
enda kwa Yoshua kambini kati-
ka Gilgali[a] na kumwambia yeye
na watu wa Israeli hivi: "Sisi tu-
metoka nchi ya mbali. Basi sasa
fanyeni agano[b] pamoja nasi."
7 Ndipo watu wa Israeli waka-
waambia hao Wahivi:[c] "Labda
mnakaa katika ujirani wetu.
Basi tunawezaje kufanya agano
pamoja nanyi?"[d] **8** Nao waka-
mwambia Yoshua: "Sisi ni watu-
mishi wako."[e]

Kisha Yoshua akawaambia:
"Ninyi ni nani, nanyi mnato-
ka wapi?" **9** Ndipo wakamwa-
mbia: "Watumishi wako wame-
toka nchi ya mbali sana[f] kwa sa-
babu ya jina[g] la Yehova Mungu
wako, kwa kuwa tumesikia sifa
zake na mambo yote ambayo
alitenda katika Misri,[h] **10** na
yote ambayo aliwatendea wale
wafalme wawili wa Waamori
waliokuwa ng'ambo ile nyingi-
ne ya Yordani, yaani, Sihoni[i]
mfalme wa Heshboni na Ogu[j]
mfalme wa Bashani, aliyekuwa
katika Ashtarothi.[k] **11** Basi
wazee wetu na wakaaji wote wa
nchi yetu wakatuambia hivi,[l]
'Chukueni chakula mikononi
mwenu kwa ajili ya safari ki-
sha mwende mkakutane nao,
nanyi mtawaambia hivi: "Sisi ni
watumishi wenu.[m] Basi sasa fa-
nyeni agano pamoja nasi."'[n]
12 Mkate wetu huu ulikuwa
moto tulipouchukua kuwa cha-
kula chetu kutoka katika nyu-
mba zetu siku ile tulipoanza
safari ya kuja hapa kwenu, na
sasa, tazama! umekauka nao
umekuwa wenye kuvunjika-vu-
njika.[o] **13** Na hivi ndivyo viri-
ba vya divai ambavyo tulivijaza
vikiwa vipya, na tazama! vime-
pasuka,[p] na mavazi haya na vi-
atu vyetu, vimechakaa kwa sa-
babu ya safari ya mbali sana."

14 Ndipo watu hao wakachukua sehemu ya vyakula vyao,
wala hawakuuliza habari kutoka katika kinywa cha Yehova.[a]
15 Naye Yoshua akafanya amani nao,[b] akafanya agano nao
ili kuwaacha waishi, kwa hiyo wakuu[c] wa kusanyiko wakawaapia.[d]
16 Na ikawa kwamba mwishoni mwa siku tatu, baada ya
kufanya agano nao, wakapata kusikia kwamba walikuwa karibu nao, na kwamba walikuwa wakikaa katika ujirani wao.
17 Ndipo wana wa Israeli wakaondoka na kwenda katika
majiji ya watu hao siku ya tatu, na majiji yao yalikuwa Gibeoni[e]
na Kefira[f] na Beerothi[g] na Kiriath-yearimu.[h] **18** Nao wana
wa Israeli hawakuwapiga, kwa sababu wakuu wa kusanyiko
walikuwa wamewaapia[i] kwa Yehova Mungu wa Israeli.[j] Na
kusanyiko lote likaanza kuwanung'unikia hao wakuu.[k]
19 Kwa hiyo wakuu wote wakaliambia kusanyiko lote: "Sisi
wenyewe tumewaapia kwa Yehova Mungu wa Israeli, na sasa
hatuna ruhusa ya kuwadhuru.[l] **20** Hili ndilo jambo tutakalo
wafanyia, kisha tuwaache waishi, ili hasira yoyote isitupate
kwa sababu ya kile kiapo ambacho tumewaapia."[m] **21** Basi
wakuu wakawaambia hivi: "Waacheni waishi, na wawe waku
sanyaji wa kuni na watekaji wa maji kwa ajili ya kusanyiko
lote,[n] kama hao wakuu walivyowaahidi."[o]
22 Basi sasa Yoshua akawaita
na kuwaambia: "Kwa nini mlitufanyia ujanja, mkisema, 'Tumetoka mbali sana na ninyi,'[p]
na kumbe mnakaa kati yetu?[q]
23 Basi sasa ninyi ni watu waliolaaniwa,[r] nanyi hamtaacha kamwe kuwa watumwa[a] na
wakusanyaji wa kuni na watekaji wa maji kwa ajili ya nyumba
ya Mungu wangu."[b] **24** Ndipo
wakamjibu Yoshua na kusema:
"Kwa sababu watumishi wako
waliambiwa waziwazi kwamba
Yehova Mungu wako alikuwa
amemwamuru Musa mtumishi
wake awape ninyi nchi yote na
kuwaangamiza wakaaji wote wa
nchi kutoka mbele yenu,[c] nasi
tukaogopa sana kwa ajili ya
nafsi zetu kwa sababu yenu.[d]
Kwa hiyo tukafanya jambo hili.[e]
25 Na sasa tupo hapa, mkononi mwako. Basi kama unavyoona kuwa ni vema na sawa
machoni pako kututendea, tutendee hivyo."[f] **26** Kwa hiyo
akawatendea hivyo na kuwakomboa kutoka mkononi mwa
wana wa Israeli, nao hawakuwaua.[g] **27** Basi Yoshua akawafanya[h] siku hiyo kuwa wa
kusanyaji wa kuni na watekaji wa maji kwa ajili ya kusanyiko[i] na kwa ajili ya madhabahu
ya Yehova, mpaka leo hii, mahali ambapo angechagua.[j]

10 Na ikawa kwamba mara
tu Adoni-sedeki mfalme
wa Yerusalemu aliposikia kwamba Yoshua ameteka Ai[k] na kuliharibu,[l] kwamba jinsi alivyofanya Yeriko[m] na mfalme wake,[n]
ndivyo alivyofanya Ai na mfalme wake,[o] na kwamba wakaaji wa Gibeoni walikuwa wamefanya amani na Israeli[p] na kuendelea kukaa katikati yao,
2 akaogopa sana,[q] kwa sababu Gibeoni lilikuwa jiji kubwa,
kama moja la majiji ya kifalme,
na kwa sababu lilikuwa kubwa
kuliko Ai,[r] na wanaume wake
wote walikuwa wenye nguvu.
3 Basi Adoni-sedeki mfalme

SURA 9

a Kut 28:30; Hes 27:21; 1Sa 30:7; Met 3:5; Met 3:6
b Yos 11:19
c Hes 34:18; 2Nya 5:2
d 2Sa 21:2
e Yos 10:2; Yos 18:25
f Ezr 2:25
g Ne 7:29
h Yos 15:9; Yos 18:14; 1Sa 7:1; 1Nya 13:5
i Hes 30:2; Mt 5:33
j Kum 6:13
k Kut 22:28; Flp 2:14
l Zb 15:4; Mhu 5:4; Mhu 5:6
m 2Sa 21:1; Met 6:17; Met 8:13; Zek 5:4; Zek 8:17; Mal 3:5
n Kum 29:11
o Yos 9:15
p Yos 9:6
q Yos 9:16
r Mwa 9:25; Mwa 9:26

Safu ya 2

a 1Fa 9:21
b Kum 29:11; Ezr 8:17
c Kut 23:31; Hes 33:52; Kum 7:1; Kum 20:16
d Kut 15:15; Kum 2:25; Kum 11:25; Yos 5:1
e Yon 3:9; Ro 3:29; Ebr 11:31
f Mwa 16:6; Amu 10:15; 2Sa 24:14; Yer 26:14
g Yer 39:18
h 1Nya 9:2; Ezr 7:24; Ezr 8:17; Ne 3:26; Ne 7:60
i Kum 29:11; Yos 9:21
j Kum 12:5; 1Fa 8:29; 2Nya 6:6

SURA 10

k Yos 8:2
l Yos 8:24
m Yos 6:21
n Yos 6:2
o Yos 8:29
p Yos 9:15; Yos 11:19
q Kut 15:16; Kum 2:25; Kum 11:25; Yos 2:11; Yos 5:1
r Yos 8:25

wa Yerusalemu[a] akatuma ujumbe kwa Hohamu mfalme wa
Hebroni[b] na kwa Piramu mfalme wa Yarmuthi[c] na kwa Yafia
mfalme wa Lakishi[d] na kwa Debiri mfalme wa Egloni,[e] akisema, **4** "Pandeni mje kwangu,
mnisaidie, tupige Gibeoni, kwa sababu wamefanya amani na
Yoshua na wana wa Israeli."[f] **5** Ndipo wakakusanyika pamoja na kupanda, wafalme watano wa Waamori,[g] mfalme wa Yerusalemu, mfalme wa Hebroni, mfalme wa Yarmuthi, mfalme wa Lakishi, mfalme wa Egloni, hao na kambi zao zote, nao wakaanza kupiga kambi juu ya Gibeoni na kupiga vita juu yake.

6 Ndipo watu wa Gibeoni wakatuma ujumbe kwa Yoshua huko Gilgali kambini,[h] wakisema: "Usiulegeze mkono wako uwaache watumwa wako.[i] Panda uje kwetu haraka, utuokoe na kutusaidia, kwa maana wafalme wote wa Waamori wanaokaa katika eneo lenye milima wamekusanyika pamoja kutupiga sisi." **7** Basi Yoshua akapanda kutoka Gilgali, yeye na watu wote wa vita pamoja naye na mashujaa wote,[j] wanaume wenye nguvu.[k]

8 Ndipo Yehova akamwambia Yoshua: "Usiwaogope,[l] kwa maana nimewatia hao mkononi mwako.[m] Hakuna mtu yeyote kati yao atakayesimama juu yako."[n] **9** Ndipo Yoshua akaja juu yao kwa ghafula. Alikuwa amepanda kutoka Gilgali usiku kucha. **10** Yehova naye akawavuruga mbele ya Israeli,[o] nao wakaanza kuwaua kwa mauaji makuu katika Gibeoni,[p] wakawafuatilia kwa njia ya mpando wa Beth-horoni, wakawaua mpaka Azeka[q] na Makeda.[r] **11** Na ikawa kwamba walipokuwa wanakimbia kutoka mbele ya Israeli, wakiwa kwenye mteremko wa Beth-horoni, Yehova akawatupia mawe[a] makubwa kutoka mbinguni mpaka Azeka, nao wakafa. Wale waliokufa kutokana na hayo mawe ya mvua walikuwa wengi kuliko wale ambao wana wa Israeli waliwaua kwa upanga.

12 Ndipo Yoshua akaanza kusema na Yehova siku ile ambayo Yehova aliwatia Waamori mikononi mwa wana wa Israeli, naye akasema machoni pa Israeli:

> "Ewe jua,[b] simama tuli juu ya Gibeoni,[c]
> Nawe mwezi, juu ya nchi tambarare ya chini ya Aiyaloni."[d]

13 Basi jua likasimama tuli, mwezi nao ukasimama, mpaka taifa hilo lilipokuwa limelipiza kisasi juu ya adui zake.[e] Je, habari hizo hazikuandikwa katika kitabu cha Yashari?[f] Na jua likaendelea kusimama katikati ya mbingu nalo halikuharakisha kwenda kutua kwa karibu siku nzima.[g] **14** Na hakuna siku ambayo imepata kuwa kama hiyo, wala kabla yake wala baada yake, kwa kuwa Yehova aliisikia sauti ya mwanadamu,[h] kwa maana Yehova mwenyewe alikuwa akipigania Israeli.[i]

15 Baadaye Yoshua na Israeli wote pamoja naye wakarudi kambini huko Gilgali.[j]

16 Wakati huohuo wale wafalme watano wakakimbia,[k] wakaenda kujificha katika pango huko Makeda.[l] **17** Ndipo Yoshua akapata habari, ikisema: "Wale wafalme watano wamepatikana wakiwa wamejificha katika pango kule Makeda."[m] **18** Basi Yoshua akasema: "Viringisheni mawe makubwa ka-

SURA 10

a Yos 12:10
Yos 18:28
b Mwa 23:2
Hes 13:22
c Yos 12:11
d 2Fa 18:14
e Yos 12:12
Yos 15:39
f Yos 9:15
Yos 11:19
g Mwa 15:16
h Yos 5:10
Yos 9:6
i Yos 9:15
Yos 9:25
j Yos 8:1
k Yos 8:3
l Kum 3:2
Kum 20:1
m Kum 7:24
Yos 11:6
n Yos 1:5
o Zb 44:3
Zb 78:55
p Isa 28:21
q Yos 15:35
r Yos 15:41

Safu ya 2

a Ayu 38:22
Zb 18:13
Zb 148:8
Isa 30:30
b Mwa 1:16
2Fa 20:10
Zb 135:6
Isa 38:8
c Isa 28:21
d Yos 19:42
e Yos 21:44
f 2Sa 1:18
g Zb 74:16
Zb 135:6
Zb 136:8
Mt 19:26
h Kum 9:19
1Fa 17:22
Zb 113:6
Yak 5:16
i Kut 14:14
Kum 1:30
Kum 3:22
Yos 23:3
Zb 33:20
Isa 42:13
Zek 14:3
j Yos 5:10
Yos 9:6
k Zb 48:5
l Yos 10:10
m Yos 10:28
Zb 139:7
Amo 9:3

tika kinywa cha pango hilo na kuweka watu juu ya pango hilo wawalinde. **19** Lakini ninyi msisimame. Wafuatilieni adui zenu, nanyi mwapige upande wa nyuma.[a] Msiwaache waingie katika majiji yao, kwa kuwa Yehova Mungu wenu amewatia mikononi mwenu."[b]

20 Na ikawa kwamba mara tu Yoshua na wana wa Israeli walipomaliza kuwaua kwa mauaji makubwa sana, mpaka wakakomeshwa,[c] na wale waliobaki kati yao wakakimbia na kuingia katika majiji yenye ngome,[d] **21** watu wote wakaanza kurudi kwa amani kambini, kwa Yoshua, katika Makeda. Hakuna mtu yeyote aliyeutoa ulimi wake kinyume cha wana wa Israeli.[e] **22** Ndipo Yoshua akasema: "Fungueni kinywa cha pango, watoeni hawa wafalme watano kutoka ndani ya pango, mkawalete kwangu." **23** Basi wakafanya hivyo, wakawatoa hao wafalme watano ndani ya pango, wakawaleta kwake, mfalme wa Yerusalemu,[f] mfalme wa Hebroni,[g] mfalme wa Yarmuthi, mfalme wa Lakishi,[h] mfalme wa Egloni.[i] **24** Na ikawa kwamba mara tu walipokuwa wamewaleta wafalme hao kwa Yoshua, Yoshua akawaita wanaume wote wa Israeli na kuwaambia viongozi wa wanaume wa vita waliokuwa wameenda pamoja naye: "Haya, sogeeni mbele. Wekeni nyayo za miguu yenu upande wa nyuma wa shingo za wafalme hawa."[j] Basi wakasogea mbele, wakaweka nyayo za miguu yao upande wa nyuma wa shingo zao.[k] **25** Tena Yoshua akawaambia: "Msiogope wala msiingiwe na hofu.[l] Iweni hodari na wenye nguvu, kwa maana hivi ndivyo Yehova atakavyowatendea adui zenu wote ambao mnapigana vita nao."[a]

26 Kisha Yoshua akawapiga na kuwaua, akawatundika juu ya miti mitano, nao wakaendelea kuning'inia juu ya miti hiyo mpaka jioni.[b] **27** Na ikawa kwamba Yoshua akatoa amri wakati wa kutua kwa jua, nao wakawashusha kutoka juu ya miti[c] hiyo na kuwatupa ndani ya pango ambamo walikuwa wamejificha. Kisha wakaweka mawe makubwa katika kinywa cha pango hilo—mpaka leo hii.

28 Na Yoshua akateka Makeda[d] siku hiyo, akalipiga kwa makali ya upanga. Naye akamwangamiza mfalme wake na kila nafsi iliyokuwamo ndani yake.[e] Hakuacha mtu yeyote aokoke. Kwa hiyo akamtendea mfalme wa Makeda[f] kama vile alivyomtendea mfalme wa Yeriko.

29 Kisha Yoshua na Israeli wote pamoja naye wakapita kutoka Makeda mpaka Libna, wakapiga vita juu ya Libna.[g] **30** Basi Yehova akalitia jiji hilo na mfalme wake pia mkononi mwa Israeli, nao wakalipiga jiji hilo na kila nafsi iliyokuwa ndani yake kwa makali ya upanga. Hawakuacha mtu yeyote aokoke ndani yake. Kwa hiyo wakamtendea mfalme wake kama vile walivyomtendea mfalme wa Yeriko.[h]

31 Kisha Yoshua na Israeli wote pamoja naye wakapita kutoka Libna mpaka Lakishi,[i] wakapiga kambi juu yake na kupiga vita juu yake. **32** Kwa hiyo Yehova akatia Lakishi mkononi mwa Israeli, nao wakaliteka siku ya pili, wakalipiga kwa makali ya upanga na pia kila nafsi iliyokuwa ndani yake,[j] kulingana na yote ambayo walikuwa wamelitendea Libna.

SURA 10

a Kum 28:7
b Law 26:8
Ne 9:24
c Yos 8:24
d 2Sa 20:6
e Kut 11:7
f Yos 10:3
Yos 12:10
g Yos 15:13
h Yos 12:11
i Yos 10:5
Yos 12:12
j Mwa 49:8
2Sa 22:41
Zb 18:40
k Kut 23:27
Kum 33:29
Zb 110:1
l Kum 1:29
Kum 31:6
Yos 1:9
Zb 27:14

Safu ya 2

a Kum 3:21
Kum 7:19
b Kum 21:22
c Kum 21:23
Yos 8:29
d Yos 10:10
Yos 12:16
Yos 15:41
e Law 27:29
Kum 20:16
Zb 21:8
f Yos 12:16
g Yos 12:15
Yos 15:42
Yos 21:13
h Yos 6:21
Yos 8:2
Yos 8:29
i Yos 10:3
Yos 12:11
Yos 15:39
j Kum 7:2
Kum 20:16

33 Ndipo Horamu mfalme wa Gezeri[a] akapanda kusaidia Lakishi. Basi Yoshua akampiga yeye na watu wake hata hakuacha mtu yeyote wake aokoke.[b]

34 Kisha Yoshua na Israeli wote wakapita kutoka Lakishi mpaka Egloni,[c] wakapiga kambi juu yake na kupiga vita juu yake. **35** Nao wakaliteka siku hiyo na kuanza kulipiga kwa makali ya upanga, wakaangamiza siku hiyo kila nafsi iliyokuwa ndani yake, kulingana na yote ambayo walikuwa wamelitendea Lakishi.[d]

36 Kisha Yoshua na Israeli wote pamoja naye wakapanda kutoka Egloni mpaka Hebroni,[e] wakaanza kupiga vita juu yake. **37** Nao wakaliteka, wakalipiga pamoja na mfalme wake na miji yake yote na kila nafsi iliyokuwa ndani yake kwa makali ya upanga. Hakuacha mtu yeyote aokoke, kulingana na yote aliyokuwa amelitendea Egloni. Kwa hiyo akaliangamiza[f] pamoja na kila nafsi iliyokuwa ndani yake.

38 Mwishowe Yoshua na Israeli wote pamoja naye wakarudi Debiri,[g] wakaanza kupiga vita juu yake. **39** Naye akaliteka pamoja na mfalme wake na miji yake yote, wakawapiga kwa makali ya upanga na kuangamiza[h] kila nafsi iliyokuwa ndani yake. Hakuacha mtu yeyote aokoke.[i] Kulingana na vile alivyolitendea Hebroni, ndivyo alivyolitendea Debiri na mfalme wake, na kama vile alivyolitendea Libna na mfalme wake.[j]

40 Na Yoshua akaanza kuipiga nchi yote ya eneo lenye milima[k] na Negebu[l] na Shefela[m] na miteremko[n] na wafalme wao wote. Hakuacha mtu yeyote aokoke,[o] akaangamiza[p] kila kitu kilichopumua, kama vile Yehova Mungu wa Israeli alivyokuwa ameamuru.[a] **41** Naye Yoshua akawapiga kutoka Kadeshbarnea[b] mpaka Gaza[c] na nchi yote ya Gosheni[d] kufika Gibeoni.[e] **42** Na Yoshua akateka wafalme hao wote na nchi zao wakati mmoja,[f] kwa kuwa ni Yehova Mungu wa Israeli aliyekuwa akipigania Israeli.[g] **43** Baada ya hayo Yoshua na Israeli wote pamoja naye wakarudi kambini huko Gilgali.[h]

11 Na ikawa kwamba mara tu Yabini mfalme wa Hasori aliposikia habari hizo, akatuma ujumbe kwa Yobabu mfalme wa Madoni[i] na kwa mfalme wa Shimroni na mfalme wa Akshafi,[j] **2** na kwa wafalme waliokuwa upande wa kaskazini katika eneo lenye milima na katika nchi tambarare za jangwa upande wa kusini wa Kinerethi[k] na katika Shefela[l] na katika safu za milima ya Dori[m] upande wa magharibi, **3** Wakanaani[n] upande wa mashariki na magharibi, na Waamori[o] na Wahiti[p] na Waperizi[q] na Wayebusi[r] katika eneo lenye milima na Wahivi,[s] pale chini ya Hermoni[t] katika nchi ya Mispa.[u] **4** Basi wakatoka, wao na kambi zao zote pamoja nao, hesabu kubwa sana ya watu kama chembe za mchanga ulio kando ya bahari kwa wingi,[v] na farasi[w] wengi sana na magari ya vita. **5** Ndipo wafalme hao wote wakakutana pamoja kwa mapatano, wakaja na kupiga kambi pamoja kando ya maji ya Meromu ili kupigana na Israeli.[x]

6 Ndipo Yehova akamwambia Yoshua: "Usiogope kwa sababu yao,[y] kwa maana kesho karibu wakati kama huu nitawatoa wote kwa Israeli wa-

SURA 10

a Yos 12:12
Yos 16:10
Yos 21:21
Amu 1:29
1Fa 9:16
b Law 27:29
c Yos 10:3
Yos 12:12
Yos 15:39
d Kum 20:16
Yos 10:32
e Mwa 13:18
Mwa 23:19
Hes 13:22
Yos 10:3
Yos 14:13
Yos 15:13
Yos 21:13
Amu 1:10
f Law 27:29
Yos 6:21
g Yos 12:13
Yos 15:15
Amu 1:11
h Kum 7:2
Kum 20:16
i Yos 11:14
j Yos 10:30
Yos 10:32
k Kum 1:7
l Mwa 20:1
m Yos 9:1
Yos 15:33
Amu 1:9
n Yos 12:8
o Law 27:29
p Kum 20:16
Yos 11:14

Safu ya 2

a Kum 7:2
Kum 9:5
b Hes 34:4
Kum 9:23
Yos 15:3
c Mwa 10:19
Kum 2:23
d Yos 11:16
Yos 15:51
e Yos 11:19
f Yos 11:18
g Kut 14:14
Kum 1:30
Kum 3:22
h Yos 4:19

SURA 11

i Yos 12:19
j Yos 12:20
k Hes 34:11
l Yos 10:40
m Yos 12:23
Yos 17:11
Amu 1:27
n Kum 20:17
o Mwa 15:16
Amo 2:9
p Kum 7:1
q Kut 3:8
r Hes 13:29
s Amu 3:3
t Kum 4:48
Yos 13:11
u Yos 11:8
v 1Sa 13:5
w Zb 33:17
Met 21:31
x Zb 3:6
Zb 118:10
y Yos 10:8
Zb 27:1
Zb 46:1

kiwa wamechinjwa. Mtawalemaza farasi wao kwa kuwakata mishipa ya upande wa nyuma wa magoti,[a] nayo magari yao mtayateketeza kwa moto."[b]
7 Na Yoshua na watu wote wa vita pamoja naye wakaja juu yao kwa ghafula kando ya maji ya Meromu, wakawaangukia.
8 Ndipo Yehova akawatia mkononi[c] mwa Israeli, nao wakawapiga na kuwafuatilia mpaka Sidoni[d] jiji lenye hesabu kubwa ya watu na Misrefoth-maimu[e] na nchi tambarare ya bondeni ya Mispe[f] upande wa mashariki; nao wakaendelea kuwapiga, hata asibaki yeyote kati yao mwenye kuokoka.[g] **9** Kisha Yoshua akawatendea kama vile Yehova alivyokuwa amemwambia: akakata mishipa ya upande wa nyuma wa magoti ya farasi wao,[h] nayo magari yao akayateketeza katika moto.[i]

10 Tena Yoshua akageuka wakati huo[j] na kuteka Hasori;[k] akampiga na kumuua mfalme wake kwa upanga,[l] kwa sababu kabla ya wakati huo, Hasori lilikuwa ndilo kichwa cha falme hizo zote. **11** Nao wakaipiga kila nafsi iliyokuwa ndani yake kwa makali ya upanga, na kuwaangamiza.[m] Hakuna kitu chochote kinachopumua ambacho kilibakia,[n] naye akateketeza Hasori katika moto. **12** Na Yoshua akateka majiji yote ya wafalme hao, naye akawakamata wafalme wao wote, akawapiga kwa makali ya upanga.[o] Akawaangamiza,[p] kama vile Musa mtumishi wa Yehova alivyokuwa ameamuru.[q] **13** Majiji ambayo Israeli hawakuteketeza ni yale yote yanayosimama juu ya vilima vyao peke yake, ila Yoshua aliteketeza jiji la Hasori tu. **14** Na wana wa Israeli wakapora kwa ajili yao wenyewe nyara zote za majiji hayo na wanyama wa kufugwa.[a] Walipiga kwa makali ya upanga binadamu wote peke yao, mpaka walipokuwa wamewaangamiza.[b] Hawakuacha yeyote anayepumua abaki.[c] **15** Kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa mtumishi wake, ndivyo Musa alivyomwamuru Yoshua,[d] na ndivyo Yoshua alivyofanya. Hakuondoa hata neno moja kutoka kwa yote ambayo Yehova alikuwa amemwamuru Musa.[e]

16 Na Yoshua akachukua nchi hiyo yote, eneo lenye milima na Negebu[f] yote na nchi yote ya Gosheni[g] na Shefela[h] na Araba[i] na eneo lenye milima la Israeli na Shefela yake,[j] **17** kutoka Mlima Halaki,[k] unaopanda mpaka Seiri,[l] na mpaka Baal-gadi[m] katika nchi tambarare ya bondeni ya Lebanoni, pale chini ya Mlima Hermoni,[n] naye akawakamata wafalme wao wote, akawapiga na kuwaua.[o] **18** Yoshua alipiga vita na wafalme hao wote kwa siku nyingi. **19** Hakuna jiji lolote lililofanya amani na wana wa Israeli isipokuwa Wahivi[p] wanaokaa Gibeoni.[q] Majiji mengine yote waliyachukua kwa vita.[r] **20** Kwa kuwa hiyo ndiyo iliyokuwa njia ya Yehova ya kutenda, kuacha mioyo yao iwe migumu[s] ili watangaze vita juu ya Israeli, kusudi awaangamize, ili wasipate kibali,[t] bali ili yeye apate kuwaangamiza, kama vile Yehova alivyokuwa amemwamuru Musa.[u]

21 Na zaidi ya hayo, Yoshua, wakati uleule, akaenda na kuwakatilia mbali Waanaki[v] kutoka katika eneo lenye milima,

SURA 11

a Kum 17:16
Yos 11:9
2Sa 8:4
b Zb 20:7
Isa 31:1
c Yos 21:44
Yos 23:10
Ne 9:24
d Mwa 10:19
Yos 19:28
e Yos 13:6
f Yos 11:3
g Kum 20:16
h Kum 17:16
Yos 11:6
i Isa 31:1
j Yos 11:18
k Yos 19:36
l Yos 12:19
Zb 136:17
m Law 27:29
Yos 11:14
n Kum 20:16
Yos 10:40
o Kum 9:5
p Kum 7:16
Yos 11:20
q Hes 33:52
Kum 7:2
Yos 9:24

Safu ya 2

a Hes 31:23
Kum 20:16
Yos 8:2
Yos 8:27
b Kum 7:2
c Kum 20:16
d Kum 3:28
Kum 4:5
Kum 7:1
Kum 31:7
e Kum 4:2
Kum 12:32
Zb 119:4
f Hes 13:17
Kum 1:7
Yos 10:40
Yos 12:8
g Yos 10:41
Yos 15:51
h Amu 1:9
i Kum 3:17
Yos 12:1
Yos 12:8
Yos 18:18
j Yos 9:1
k Yos 12:7
l Mwa 32:3
Kum 2:1
m Yos 13:5
n Kum 4:48
Yos 13:11
o Kum 7:24
Zb 136:18
p Yos 9:7
q Yos 9:15
Yos 10:4
r Kum 20:17
s Kum 2:30
Ro 9:18
t Kut 34:12
Kum 7:2
u Kum 20:16
Yos 11:14
v Hes 13:22
Kum 1:28
Yos 15:13

kutoka Hebroni, kutoka Debiri, kutoka Anabu[a] na kutoka katika eneo lote lenye milima la Yuda na kutoka katika eneo lote lenye milima la Israeli.[b] Yoshua akawaangamiza[c] pamoja na majiji yao. **22** Hakuna Waanaki wowote walioachwa katika nchi ya wana wa Israeli. Walibaki[d] tu katika Gaza,[e] katika Gathi[f] na katika Ashdodi.[g] **23** Basi Yoshua akaichukua nchi yote, kulingana na yote ambayo Yehova alikuwa amemwahidi Musa,[h] kisha Yoshua akawapa Israeli iwe urithi wao kulingana na mafungu yao, kulingana na makabila yao.[i] Na nchi haikusumbuliwa na vita tena.[j]

12 Basi hawa ndio wafalme wa nchi ambao wana wa Israeli waliwashinda, na kuimiliki nchi yao ng'ambo ya Yordani upande wa mapambazuko ya jua,[k] kutoka bonde la mto la Arnoni[l] hadi Mlima Hermoni[m] na Araba[n] yote upande wa mashariki: **2** Sihoni[o] mfalme wa Waamori, aliyekaa katika Heshboni,[p] akitawala kutoka Aroeri,[q] lililokuwa kwenye ukingo wa bonde la mto la Arnoni,[r] na katikati ya bonde la mto, na nusu ya Gileadi hadi bonde la mto la Yaboki,[s] mpaka wa wana wa Amoni, **3** na Araba[t] hadi bahari ya Kinerethi[u] kuelekea mashariki hadi bahari ya Araba, yaani, Bahari ya Chumvi,[v] upande wa mashariki kuelekea Beth-yeshimothi,[w] na kuelekea kusini chini ya miteremko ya Pisga.[x]

4 Na eneo la Ogu[y] mfalme wa Bashani, lile lililobaki la Warefaimu,[z] waliokaa katika Ashtarothi[a] na Edrei,[b] **5** na waliotawala katika Mlima Hermoni[c] na katika Saleka na katika Bashani[d] yote, hadi mpaka wa Wageshuri[a] na Wamaakathi,[b] na nusu ya Gileadi, hadi katika eneo la Sihoni[c] mfalme wa Heshboni.[d]

6 Musa mtumishi wa Yehova na wana wa Israeli ndio waliowashinda,[e] kisha Musa mtumishi wa Yehova akawapa Warubeni[f] na Wagadi[g] na nusu ya kabila la Manase[h] iwe urithi wao.

7 Na hawa ndio wafalme wa nchi ambao Yoshua na wana wa Israeli waliwashinda ng'ambo ya Yordani kuelekea magharibi, kuanzia Baal-gadi[i] katika nchi tambarare ya bondeni ya Lebanoni[j] hadi Mlima Halaki,[k] unaopanda hadi Seiri,[l] kisha Yoshua akawapa makabila ya Israeli iwe urithi wao kulingana na mafungu yao,[m] **8** katika eneo lenye milima na katika Shefela na katika Araba na kwenye miteremko na katika nyika na katika Negebu[n]—Wahiti, Waamori[o] na Wakanaani, Waperizi, Wahivi na Wayebusi:[p]

9 Mfalme wa Yeriko,[q] mmoja; mfalme wa Ai,[r] jiji lililokuwa kando ya Betheli, mmoja;
10 mfalme wa Yerusalemu,[s] mmoja; mfalme wa Hebroni,[t] mmoja;
11 mfalme wa Yarmuthi,[u] mmoja; mfalme wa Lakishi,[v] mmoja;
12 mfalme wa Egloni,[w] mmoja; mfalme wa Gezeri,[x] mmoja;
13 mfalme wa Debiri,[y] mmoja; mfalme wa Gederi, mmoja;
14 mfalme wa Horma, mmoja; mfalme wa Aradi, mmoja;

SURA 11
a Yos 15:50
b Yos 11:16
c Law 27:29; Yos 11:12; Yos 24:11
d Kut 23:29; Kut 23:30; Zb 105:44
e Yos 10:41; Amu 1:18
f 1Sa 17:4
g Yos 15:46; 2Nya 26:6; Ne 13:23
h Kut 23:27; Hes 34:2; Kum 11:23
i Hes 26:53; Yos 14:1; Yos 15:1; Yos 16:1; Yos 17:1
j Yos 14:15; Yos 21:44; Yos 23:1; Zb 29:11; Met 16:7

SURA 12
k Kum 4:47; Yos 1:15
l Hes 21:24; Kum 2:24
m Kum 3:8; Kum 4:48
n Kum 4:49
o Hes 21:23; Ne 9:22
p Kum 2:26
q Kum 3:12; Amu 11:26
r Hes 21:13; Yos 13:9
s Amu 11:13
t Kum 3:17
u Yoh 6:1
v Yos 3:16
w Yos 13:20
x Kum 3:27
y Hes 21:33; Kum 3:1
z Kum 3:11; Yos 13:12
a Kum 1:4
b Kum 3:10
c Yos 12:1
d Kum 29:7; Yos 9:10

Safu ya 2
a Kum 3:14
b Yos 13:13
c Yos 12:2
d Hes 21:26; Kum 3:6
e Hes 21:24; Hes 21:35
f Kum 3:12
g Hes 32:33
h Kum 3:13
i Yos 13:5
j Yos 1:4
k Yos 11:17
l Kum 2:12
m Yos 11:23
n Yos 10:40; Yos 11:16
o Mwa 15:16; Kut 3:8; Zb 136:19
p Kut 23:23; Kum 7:1
q Yos 6:2

r Yos 8:29; s Yos 10:1; t Yos 10:23; u Yos 10:3; v Yos 10:23; w Yos 10:23; x Yos 10:33; y Yos 10:38.

15 mfalme wa Libna,[a] mmoja; mfalme wa Adulamu, mmoja;
16 mfalme wa Makeda,[b] mmoja; mfalme wa Betheli,[c] mmoja;
17 mfalme wa Tapua, mmoja; mfalme wa Heferi,[d] mmoja;
18 mfalme wa Afeki, mmoja; mfalme wa Lasharoni, mmoja;
19 mfalme wa Madoni,[e] mmoja; mfalme wa Hasori,[f] mmoja;
20 mfalme wa Shimron-meroni, mmoja; mfalme wa Akshafi,[g] mmoja;
21 mfalme wa Taanaki, mmoja; mfalme wa Megido,[h] mmoja;
22 mfalme wa Kedeshi, mmoja; mfalme wa Yokneamu[i] katika Karmeli, mmoja;
23 mfalme wa Dori katika safu ya milima ya Dori,[j] mmoja; mfalme wa Goimu katika Gilgali, mmoja;
24 mfalme wa Tirsa, mmoja; wafalme wote walikuwa 31.[k]

13 Basi Yoshua alikuwa mzee, amesonga katika miaka.[l] Kwa hiyo Yehova akamwambia: "Wewe mwenyewe umezeeka na kusonga katika miaka, na sehemu kubwa ya nchi bado haijamilikiwa.[m] **2** Hii ndiyo nchi ambayo bado imebaki:[n] maeneo yote ya Wafilisti[o] na Wageshuri[p] wote **3** (kutoka kile kijito cha Nile kilichoko mbele ya Misri hadi kwenye mpaka wa Ekroni upande wa kaskazini,[q] ilikuwa ikihesabiwa kuwa ni ya Wakanaani);[r] wakuu watano[s] wa muungano wa Wafilisti, Wagaza[t] na Waashdodi,[u] Waashkeloni,[v] Wagathi[a] na Waekroni;[b] na Waavimu.[c] **4** Upande wa kusini, nchi yote ya Wakanaani; na Meara, ambayo ni ya Wasidoni,[d] hadi Afeki, hadi mpaka wa Waamori; **5** na nchi ya Wagebali[e] na Lebanoni yote upande wa mapambazuko ya jua, kuanzia Baal-gadi[f] ulio chini ya Mlima Hermoni hadi maingilio ya Hamathi;[g] **6** wakaaji wote wa eneo lenye milima, kutoka Lebanoni[h] hadi Misrefoth-maimu,[i] Wasidoni[j] wote; mimi mwenyewe nitawanyang'anya nchi na kuwafukuza mbele ya wana wa Israeli.[k] Uwawezeshe wana wa Israeli kuirithi, kama vile ambavyo nimekuamuru.[l] **7** Na sasa igawe nchi hii iwe urithi kwa yale makabila tisa na kwa ile nusu ya kabila la Manase."[m]

8 Na pamoja na ile nusu nyingine ya kabila, Warubeni na Wagadi walichukua urithi wao ambao Musa aliwapa ng'ambo ya Yordani iliyo upande wa mashariki, kama vile Musa mtumishi wa Yehova alivyokuwa amewapa,[n] **9** kutoka Aroeri,[o] lililo kwenye ukingo wa bonde la mto la Arnoni,[p] na lile jiji lililo katikati ya hilo bonde la mto, na nchi yote tambarare ya juu ya Medeba[q] hadi Diboni;[r] **10** na majiji yote ya Sihoni mfalme wa Waamori, aliyetawala katika Heshboni, hadi kwenye mpaka wa wana wa Amoni;[s] **11** na Gileadi na eneo la Wageshuri[t] na Wamaakathi na Mlima Hermoni[u] wote na Bashani[v] yote hadi Saleka;[w] **12** ufalme wote wa Ogu[x] katika Bashani, aliyetawala katika Ashtarothi na katika Edrei[y]—yeye ndiye aliyebaki kati ya mabaki ya Warefaimu[z]—kwa kuwa

SURA 12
a Yos 10:29
b Yos 10:28
c Yos 8:17
Amu 1:22
d 1Fa 4:10
e Yos 11:1
f Yos 11:10
g Yos 11:1
h 1Nya 7:29
i Yos 21:34
j Yos 11:2
k Kum 28:1

SURA 13
l Yos 23:1
Yos 24:29
m Yos 12:7
n Kut 23:29
o Kut 23:31
Sef 2:5
p 1Sa 27:8
q Yos 15:11
r Mwa 10:19
s Amu 3:3
1Sa 6:4
t Yos 10:41
u Yos 15:46
v Amu 14:19

Safu ya 2
a 2Sa 21:19
b 1Sa 5:10
c Kum 2:23
d Amu 1:31
e 1Fa 5:18
Eze 27:9
f Yos 11:17
g Hes 34:8
h Kum 3:25
i Yos 11:8
j Amu 3:3
k Kut 23:30
l Hes 34:17
Yos 14:1
m Hes 33:54
n Hes 32:33
Yos 22:4
o Kum 3:12
Yos 12:2
p Hes 21:13
q Hes 21:30
r Hes 32:3
s Hes 21:24
t Kum 3:14
Yos 12:5
u Kum 4:48
v Yos 17:1
w 1Nya 5:11
x Kum 3:10
y Yos 12:4
z Kum 3:11

Musa aliwapiga na kuwanyang'anya nchi na kuwafukuza.[a]
13 Na wana wa Israeli hawakuwafukuza[b] Wageshuri na Wamaakathi katika nchi, bali Geshuri[c] na Maakathi huendelea kukaa katikati ya Israeli mpaka leo hii.

14 Kabila la Walawi peke yake ndilo ambalo hakulipatia urithi.[d] Matoleo ya Yehova Mungu wa Israeli yaliyotolewa kwa njia ya moto[e] ndiyo urithi wao,[f] kama vile ambavyo amewaahidi.[g]

15 Ndipo Musa akalipatia zawadi kabila la wana wa Rubeni kulingana na familia zao, **16** na eneo lao likawa kutoka Aroeri,[h] lililo kwenye ukingo wa bonde la mto la Arnoni, na lile jiji lililo katikati ya bonde la mto, na nchi yote tambarare ya juu, karibu na Medeba;[i] **17** Heshboni[j] na miji yake yote[k] iliyo katika nchi tambarare ya juu, Diboni[l] na Bamoth-baali[m] na Beth-baal-meoni,[n] **18** na Yahazi[o] na Kedemothi[p] na Mefaathi,[q] **19** na Kiriathaimu[r] na Sibma[s] na Sereth-shahari katika mlima wa nchi tambarare ya chini, **20** na Beth-peori na miteremko ya Pisga[t] na Beth-yeshimothi,[u] **21** na majiji yote ya nchi tambarare ya juu[v] na ufalme wote wa Sihoni mfalme wa Waamori, aliyetawala katika Heshboni,[w] na ambaye Musa alimpiga na kumuua,[x] pamoja na wakuu wa Midiani, Evi na Rekemu na Suri na Huru na Reba,[y] watawala wadogo wa Sihoni, waliokuwa wakikaa katika nchi hiyo. **22** Na Balaamu mwana wa Beori,[z] yule mwaguzi,[a] wana wa Israeli wakamuua kwa upanga pamoja na watu waliouawa. **23** Na mpaka wa wana wa Rubeni ukawa Yordani; na eneo hilo likawa urithi wa wana wa Rubeni[a] kulingana na familia zao, pamoja na majiji na makao yake.

24 Tena, Musa akalipatia zawadi kabila la Gadi, wana wa Gadi kulingana na familia zao,[b] **25** na eneo lao likawa Yazeri[c] na majiji yote ya Gileadi[d] na nusu ya nchi ya wana wa Amoni[e] hadi Aroeri,[f] lililo mbele ya Raba;[g] **26** na kutoka Heshboni[h] hadi Ramath-mispe na Betonimu na kutoka Mahanaimu[i] hadi mpaka wa Debiri;[j] **27** na katika nchi tambarare ya chini Betharamu[k] na Beth-nimra[l] na Sukothi[m] na Safoni, sehemu iliyobaki ya ufalme wa Sihoni mfalme wa Heshboni,[n] mto Yordani ukawa mpaka hadi mwisho wa bahari ya Kinerethi[o] ng'ambo ya pili ya Yordani upande wa mashariki. **28** Huo ndio uliokuwa urithi wa wana wa Gadi[p] kulingana na familia zao, pamoja na majiji na makao yake.

nanyi msimwasi Yehova wala
msitufanye sisi tuasi kwa ni-
nyi kujijengea madhabahu zai-
di ya ile madhabahu ya Yeho-
va Mungu wetu.[e] **20** Je, Aka-
ni[f] mwana wa Zera siye aliye-
fanya tendo la kukosa uaminifu
kuhusiana na kile kitu kilicho-
tengwa kwa ajili ya kuharibi-
wa, na je, hasira haikuja juu ya
kusanyiko lote la Israeli?[g] Wala
yeye siye mtu peke yake aliye-
kufa katika kosa lake.'"[h]
21 Ndipo wana wa Rubeni na
wana wa Gadi na nusu ya ka-
bila la Manase wakajibu[i] na ku-
sema na vichwa vya maelfu ya
Israeli:[j] **22** "Mwenye Uwezo,[k]
Mungu,[l] Yehova, Mwenye Uwe-
zo, Mungu, Yehova,[m] yeye ana-
jua,[n] na Israeli pia atajua.[o] Iki-
wa ni kwa uasi[p] na ikiwa ni kwa
kukosa uaminifu kwa Yehova,[q]
usituokoe leo hii. **23** Kama ili-
kuwa ni kujijengea madhabahu
ili tugeuke tusimfuate Yehova,
na kama tulitaka kutoa matoleo
ya kuketetezwa na matoleo ya
nafaka juu yake,[r] na kama tu-
litaka kutoa dhabihu za ushiri-
ka juu yake, Yehova mwenyewe
atachunguza;[s] **24** au kama tu-
lifanya hivyo kutokana na ha-
ngaiko juu ya jambo lingine, tu-
kisema, 'Siku fulani, wakati
ujao, wana wenu watawaambia
wana wetu: "Je, ninyi mna nini
na Yehova Mungu wa Israeli?
25 Na kuna mpaka ambao Ye-
hova ameweka kati yetu na ni-
nyi, wana wa Rubeni na wana
wa Gadi, yaani, Yordani. Ha-
mna fungu lolote katika Yeho-
va."[t] Na wana wenu watawafa-
nya wana wetu waache kumwo-
gopa Yehova.'[a]
26 "Basi tukasema, 'Tafa-
dhali, na tuchukue hatua kwa
ajili yetu wenyewe, kwa kuije-
nga madhabahu, si kwa ajili ya
toleo la kuketetezwa wala kwa
ajili ya dhabihu, **27** bali iwe
ushahidi kati yetu[b] na ninyi na
vizazi vyetu baada yetu kwa-
mba tutafanya utumishi wa Ye-
hova mbele zake kwa matoleo
yetu ya kuketetezwa na dhabi-
hu zetu za ushirika,[c] ili wana
wenu wasiwaambie hivi wana
wetu siku fulani wakati ujao:
"Ninyi hamna fungu lolote kati-
ka Yehova."' **28** Basi tukase-
ma, 'Na itatukia kwamba waki-
tuambia hivyo sisi, na kuwaam-
bia hivyo vizazi vyetu siku
fulani wakati ujao, sisi nasi
tutasema: "Oneni mfano wa
madhabahu ya Yehova ambao
baba zetu waliufanya, si kwa
ajili ya matoleo ya kuketete-
zwa wala kwa ajili ya dhabihu,
bali huu ni ushahidi kati yetu
na ninyi."' **29** Ni jambo lisi-
loweza kuwaziwa, kwa upande
wetu, kwamba tumwasi Yehova
kwa kupenda kwetu wenyewe
na tugeuke nyuma leo tusimfu-
ate Yehova[d] kwa kujenga ma-
dhabahu kwa ajili ya matoleo ya
kuketetezwa, toleo la nafaka na
dhabihu zaidi ya ile madhabahu
ya Yehova Mungu wetu ambayo
iko mbele ya maskani yake!"[e]
30 Sasa Finehasi[f] kuhani na
wakuu wa kusanyiko[g] na vi-
chwa vya maelfu ya Israeli wa-
liokuwa pamoja naye waliposi-
kia maneno hayo ambayo wali-
sema wana wa Rubeni na wana
wa Gadi na wana wa Manase,
ikawa vema machoni pao.
31 Basi Finehasi mwana wa
Eleazari kuhani akawaambia
wana wa Rubeni na wana wa

SURA 22
a Hes 16:22
Yos 7:1
1Nya 21:14
b Law 18:25
c Hes 34:2
Yos 1:11
d Yos 18:1
e Kum 12:13
Kum 12:27
Yos 22:11
1Fa 12:28
f Yos 7:1
g Yos 7:11
Yos 7:15
h Yos 7:5
Yos 7:24
Yos 7:25
i Met 15:1
Met 18:17
j Yos 22:14
k Zb 50:1
Mdo 17:29
l Mwa 2:4
Yer 10:10
m Kut 3:15
Kut 6:3
Kum 10:17
Zb 83:18
n 1Fa 8:39
Zb 139:3
Yer 12:3
o Zb 37:6
p 1Sa 15:23
q Ayu 31:5
Zb 7:3
r Kum 12:11
Kum 12:13
s Zb 44:21
Mhu 12:14
Yer 32:19
Ebr 4:13
t 1Fa 12:16

Safu ya 2
a Kum 13:4
Mhu 8:13
b Mwa 31:48
Yos 24:27
c Kum 12:6
Kum 12:27
d Kum 6:14
e Kum 12:14
2Nya 32:12
f Yos 22:13
g Hes 1:16
Yos 22:14

Gadi na wana wa Manase: "Leo tunajua kwamba Yehova yupo katikati yetu,[a] kwa kuwa ninyi hamkufanya tendo hili la kukosa uaminifu juu ya Yehova. Basi sasa mmewakomboa wana wa Israeli kutoka katika mkono wa Yehova."[b]

32 Ndipo Finehasi mwana wa Eleazari kuhani na wale wakuu wakarudi[c] kutoka kwa wana wa Rubeni na wana wa Gadi katika nchi ya Gileadi, wakaenda katika nchi ya Kanaani kwa wale wana wengine wa Israeli, wakawaletea habari.[d] **33** Nayo habari hiyo ikawa njema machoni pa wana wa Israeli; nao wana wa Israeli wakambariki Mungu,[e] wala hawakuongea kuhusu kwenda katika utumishi wa kijeshi juu yao ili kuiharibu nchi ambayo wana wa Rubeni na wana wa Gadi walikuwa wakikaa.

34 Nao wana wa Rubeni na wana wa Gadi wakaipa madhabahu hiyo jina, kwa sababu "hiyo ni ushahidi kati yetu kwamba Yehova ndiye Mungu wa kweli."[f]

23 Na ikawa kwamba baada ya siku nyingi Yehova alipokuwa amekwisha kuwapa Israeli pumziko[g] kutoka kwa adui zao wote kuzunguka pande zote, wakati Yoshua alipokuwa mzee na mwenye siku nyingi,[h] **2** ndipo Yoshua akaita Israeli wote,[i] wanaume wao wazee na wakuu wao na waamuzi wao na maofisa wao,[j] naye akawaambia: "Mimi nimekuwa mzee, siku zangu zimekuwa nyingi. **3** Lakini ninyi, mmeona mambo yote ambayo Yehova Mungu wenu aliyatendea mataifa haya yote kwa ajili yenu,[k] kwa maana Yehova Mungu wenu ndiye aliyekuwa akiwapigania ninyi.[l] **4** Oneni, niliwagawia kwa kura[a] mataifa haya yanayobaki yawe urithi kwa ajili ya makabila yenu, na mataifa yote ambayo nilikatilia mbali,[b] kuanzia Yordani mpaka Bahari Kuu upande wa magharibi.[c] **5** Na Yehova Mungu wenu ndiye aliyeendelea kuwasukuma mbali kutoka mbele yenu,[d] naye akawanyang'anya miliki yao kwa ajili yenu, nanyi mkaimiliki nchi yao, kama vile Yehova Mungu wenu alivyokuwa amewaahidi ninyi.[e]

6 "Nanyi muwe hodari[f] sana ili mshike na kufanya yote ambayo yameandikwa katika kitabu[g] cha sheria ya Musa kwa kutogeuka kamwe kutoka ndani yake kwenda kuume wala kushoto,[h] **7** kwa kutoingia kamwe kati ya mataifa haya,[i] yaani, haya yanayobaki na ninyi. Nanyi msitaje majina ya miungu yao[j] wala kuapa kwa hiyo,[k] msiitumikie wala kuiinamia.[l] **8** Bali Yehova Mungu wenu ndiye mnayepaswa kushikamana naye,[m] kama vile ambavyo mmefanya mpaka leo hii. **9** Na Yehova atayafukuza mataifa makubwa na yenye nguvu kutoka mbele yenu.[n] (Lakini kwenu ninyi, hakuna hata mwanadamu mmoja ambaye amesimama mbele yenu mpaka leo hii.)[o] **10** Mtu mmoja tu kati yenu atafukuza elfu,[p] kwa maana Yehova Mungu wenu ndiye anayewapigania ninyi,[q] kama vile ambavyo amewaahidi ninyi.[r] **11** Nanyi lindeni nafsi zenu[s] kwa kumpenda Yehova Mungu wenu.[t]

12 "Lakini mkirudi nyuma kwa vyovyote[u] na kushikamana na mabaki ya mataifa haya,[v] yaani, haya yanayobaki na ninyi, na kufanya nao

SURA 22

a 2Nya 15:2
b Kum 1:13
c Yos 22:12
d Met 12:25
Met 25:13
e Da 2:20
f Mwa 5:22
Yos 24:1
Isa 44:8

SURA 23

g Kut 33:14
Law 26:6
Yos 21:44
h Yos 13:1
i Kum 31:28
j Kum 16:18
k Law 26:7
Kum 4:9
Yos 10:11
Yos 10:13
Yos 10:40
Yos 11:17
l Kum 20:4
Yos 10:14
Yos 10:42
Zb 44:3

Safu ya 2

a Hes 26:55
Yos 18:10
b Kum 7:1
c Yos 13:2
Yos 13:6
d Kut 23:30
Kut 33:2
Kut 34:11
Kum 11:23
e Hes 33:53
f Yos 1:7
g Kut 24:7
Kum 17:18
Kum 31:26
Yos 1:8
h Kum 5:32
Kum 12:32
Met 30:6
i Kut 23:33
Kum 7:2
Met 4:14
j Kut 23:13
k Yer 5:7
l Kut 20:5
m Kum 10:20
Kum 11:22
Yos 22:5
n Kum 11:23
o Yos 1:5
p Law 26:8
Amu 3:31
1Sa 14:6
2Sa 23:8
q Kut 23:27
Kum 3:22
Kum 20:4
Ro 8:31
r Kum 28:7
s Kum 4:9
Yos 22:5
t Kut 20:6
Kum 6:5
Mt 22:37
1Ko 8:3
u Ebr 10:38
2Pe 2:20
v Kut 23:29
Yos 13:2

mapatano ya ndoa[a] na kuingia katikati yao, nao wakiingia katikati yenu, **13** mnapaswa kujua hakika kwamba Yehova Mungu wenu hataendelea kuyanyang'anya mataifa haya miliki yao kwa ajili yenu;[b] nayo yatakuwa kwenu kama mtego na mnaso na kama kiboko mbavuni mwenu[c] na kama miiba machoni penu mpaka mtakapoangamia na kutoka katika nchi hii nzuri ambayo Yehova Mungu wenu amewapa ninyi.[d]

14 "Basi sasa, tazameni! leo mimi ninaenda katika njia ya dunia yote,[e] nanyi mnajua vema kwa mioyo yenu yote na kwa nafsi zenu zote kwamba halikukosa kutimia hata neno moja kati ya maneno yote mema ambayo Yehova Mungu wenu amewaambia ninyi. Yote yametimia kwenu. Halikukosa kutimia hata neno moja kati ya hayo.[f] **15** Na itatukia kwamba, kama vile neno lote jema ambalo Yehova Mungu wenu amewaambia ninyi limewafikia ninyi,[g] vivyo hivyo Yehova ataleta juu yenu neno lote ovu mpaka atakapokuwa amewaangamiza ninyi kutoka katika nchi hii nzuri ambayo Yehova Mungu wenu amewapa ninyi,[h] **16** kwa sababu ya kuvunja agano la Yehova Mungu wenu ambalo aliwaamuru ninyi, na kwa sababu mmeenda na kuitumikia miungu mingine na kuiinamia.[i] Na hasira ya Yehova hakika itawaka juu yenu,[j] nanyi hakika mtaangamia upesi kutoka katika hii nchi nzuri ambayo amewapa."[k]

24 Na ndipo Yoshua akakusanya pamoja makabila yote ya Israeli katika Shekemu,[l] akawaita wanaume wazee wote wa Israeli[m] na vichwa vyao na waamuzi wao na maofisa wao, nao wakasimama mbele za Mungu wa kweli.[a] **2** Naye Yoshua akawaambia watu wote: "Yehova Mungu wa Israeli amesema hivi, 'Mababu[b] zenu walikaa ng'ambo ile nyingine ya Mto[c] zamani za kale, Tera baba ya Abrahamu na baba ya Nahori,[d] nao walikuwa wakiitumikia miungu mingine.

3 "'Baada ya muda nikamchukua Abrahamu[e] babu yenu kutoka ng'ambo ile nyingine ya Mto,[f] nikamtembeza katika nchi yote ya Kanaani na kuufanya uzao wake kuwa mwingi.[g] Basi nikampa Isaka.[h] **4** Ndipo Isaka nikampa Yakobo na Esau.[i] Baadaye Esau nikampa Mlima Seiri ili aumiliki;[j] na Yakobo na wanawe wakashuka Misri.[k] **5** Baadaye nikamtuma Musa na Haruni,[l] nami nikapiga Misri kwa yale niliyofanya katikati yake;[m] kisha nikawatoa ninyi.[n] **6** Nilipokuwa nikiwatoa baba zenu kutoka Misri[o] nanyi mkaja kwenye ile bahari, ndipo Wamisri walipowafuatilia[p] baba zenu wakiwa na magari ya vita na wapanda-farasi mpaka kwenye Bahari Nyekundu. **7** Nao wakaanza kumlilia Yehova.[q] Basi akaweka giza kati yenu na Wamisri,[r] naye akaleta bahari juu yao na kuwafunika,[s] na macho yenu yakaona mambo niliyoyafanya huko Misri;[t] nanyi mkaanza kukaa katika nyika siku nyingi.[u]

8 "'Mwishowe nikawaleta ninyi katika nchi ya Waamori waliokuwa wakikaa ng'ambo ile nyingine ya Yordani, nao wakaanza kupigana nanyi.[v] Ndipo nikawatia mkononi mwenu ili kumiliki nchi yao, nami nikawaangamiza kutoka mbele yenu.[w] **9** Kisha Balaki mwana wa Sipo-

SURA 23

a Kut 34:16; Kum 7:3; Amu 3:6; 1Fa 11:4; Ezr 9:2; Ne 13:23
b Amu 2:3; Amu 2:21; Amu 3:8
c Hes 33:55; Kum 7:16
d Kum 4:26; Kum 28:63
e 1Fa 2:2; Mhu 9:10
f Yos 21:45; 1Fa 8:56
g Law 26:3; Kum 28:1
h Law 26:14; Kum 28:15; Kum 28:63; 2Nya 36:16; Lu 21:24
i Amu 3:6; Zb 106:36; Yer 5:19
j 2Fa 24:20
k Yos 23:13

SURA 24

l 1Fa 12:1
m Kut 18:25; Hes 1:16; Yos 23:2

Safu ya 2

a Isa 44:8; 1Ko 8:4
b Mwa 11:26
c Mwa 11:28; Mwa 11:31; Mwa 15:18; Yos 24:15
d Mwa 11:27
e Mwa 12:1; Ne 9:7; Mdo 7:2
f Yos 1:4
g Mwa 15:5; Ro 4:18; Ebr 6:14
h Mwa 21:3; Zb 127:3
i Mwa 25:26
j Mwa 36:8; Kum 2:5
k Mwa 46:3; Zb 105:23; Mdo 7:15
l Kut 3:10
m Kut 11:1
n Zb 78:52
o Kut 12:37; Mik 6:4
p Kut 14:9
q Kut 14:10
r Kut 14:20; Zb 78:14; Zb 105:39
s Kut 14:27; Zb 78:53; Zb 106:11; Zb 136:15
t Kut 3:20; Kum 4:34
u Hes 14:34; Mdo 13:18
v Hes 21:23
w Ne 9:22; Zb 135:11

ri,[a] mfalme wa Moabu, akasimama na kupigana na Israeli.[b] Basi akatuma ujumbe na kumwita Balaamu mwana wa Beori ili awalaani ninyi.[c] **10** Nami sikutaka kumsikiliza Balaamu.[d] Basi akawabariki ninyi tena na tena.[e] Hivyo nikawakomboa kutoka mkononi mwake.[f]

11 "'Kisha mkavuka Yordani,[g] mkaja Yeriko.[h] Nao wenye mashamba wa Yeriko, Waamori na Waperizi na Wakanaani na Wahiti na Wagirgashi, na Wahivi na Wayebusi wakaanza kupigana nanyi; lakini nikawatia mkononi mwenu.[i] **12** Basi nikapeleka hisia ya kuvunjika moyo mbele yenu, nayo mwishowe ikawafukuza mbele yenu[j]—wafalme wawili wa Waamori—haikuwa kwa upanga wenu wala kwa upinde wenu.[k] **13** Hivyo nikawapa ninyi nchi ambayo hamkuifanyia kazi ya taabu na majiji ambayo hamkuyajenga,[l] nanyi mkakaa ndani yake. Mashamba ya mizabibu na ya mizeituni ambayo hamkupanda ndiyo mnayokula.'[m]

14 "Na sasa mwogopeni Yehova[n] na kumtumikia kwa njia isiyo na kosa na katika kweli,[o] nanyi ondoeni miungu ambayo mababu zenu waliitumikia ng'ambo ile nyingine ya Mto na katika Misri,[p] mkamtumikie Yehova. **15** Sasa ikiwa mnaona ni vibaya machoni penu kumtumikia Yehova, jichagulieni leo yule mtakayemtumikia,[q] kama ni miungu ambayo waliitumikia[r] mababu zenu waliokuwa ng'ambo ile nyingine ya Mto au kama ni miungu ya Waamori ambao mnakaa katika nchi yao.[s] Lakini mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Yehova."[t]

16 Ndipo watu wakajibu na kusema: "Ni jambo lisilowaziwa, kwa upande wetu, kumwacha Yehova ili kuitumikia miungu mingine. **17** Kwa maana Yehova Mungu wetu ndiye aliyetuleta sisi na mababu zetu kutoka katika nchi ya Misri,[a] kutoka katika nyumba ya watumwa,[b] na ambaye alifanya ishara hizi kubwa mbele ya macho yetu,[c] akaendelea kutulinda katika njia yote ambayo tulitembea na kati ya watu wote ambao tulipita katikati yao.[d] **18** Na Yehova akafukuza vikundi vyote vya watu mbele yetu,[e] ndiyo, Waamori, waliokaa mbele yetu katika nchi. Na kwa habari yetu pia, sisi tutamtumikia Yehova, kwa maana yeye ndiye Mungu wetu."[f]

19 Ndipo Yoshua akawaambia watu: "Ninyi hamwezi kumtumikia Yehova, kwa maana yeye ni Mungu mtakatifu;[g] yeye ni Mungu anayetaka watu wajitoe kikamili.[h] Hatasamehe maasi yenu wala dhambi zenu.[i] **20** Mkimwacha Yehova[j] na kuitumikia miungu ya kigeni,[k] yeye hakika atageuka na kuwatendea ninyi madhara na kuwaangamiza baada ya kuwatendea mema."[l]

21 Nao watu wakamwambia Yoshua: "Hapana, lakini tutamtumikia Yehova!"[m] **22** Ndipo Yoshua akawaambia watu: "Ninyi ni mashahidi dhidi yenu wenyewe[n] kwamba mmemchagua Yehova kwa kupenda kwenu wenyewe, ili kumtumikia yeye."[o] Na kwa neno hilo wakajibu: "Sisi ni mashahidi."

23 "Na sasa ondoeni miungu ya kigeni iliyo katikati yenu,[p] mwelekeze mioyo yenu kwa Yehova Mungu wa Israeli." **24** Ndipo watu hao wakamwambia

SURA 24

a Hes 22:2
b Amu 11:25
c Hes 22:5
Kum 23:4
d Hes 22:12
Mik 6:5
e Hes 23:11
Hes 23:25
Hes 24:10
f Mwa 12:3
Hes 25:17
Hes 31:7
Hes 31:49
g Yos 3:17
Zb 114:3
h Yos 5:10
i Yos 11:16
Yos 21:44
Ne 9:24
Zb 78:55
Zb 105:44
Mdo 7:45
Mdo 13:19
Ebr 11:30
j Kut 23:28
Kum 7:20
Yos 2:9
k Zb 44:3
l Kum 6:10
Yos 11:14
Met 13:22
m Kum 6:11
Kum 8:8
n Kum 10:12
1Sa 12:24
Mdo 9:31
o Mwa 17:1
Kum 18:13
Zb 119:80
Yoh 4:24
p Law 17:7
Eze 23:8
q Kum 30:19
1Fa 18:21
r Yos 24:2
s Kut 23:32
Kum 7:25
Kum 13:7
Amu 6:10
Amu 10:6
t Mwa 18:19
Kum 30:19

Safu ya 2

a Kut 19:4
Kum 32:12
Amo 2:10
b Kum 6:12
1Sa 2:27
c Kut 14:31
Kum 4:34
Kum 29:2
d Kut 23:23
e Yos 24:8
f Kut 15:2
Yos 24:15
Mik 4:5
g Law 19:2
1Sa 6:20
Zb 99:5
Isa 6:3
1Pe 1:15
h Kut 20:5
Kut 34:14
Hes 25:11
Kum 6:13
Nah 1:2
Mt 4:10
i Kut 23:21
Hes 14:35
1Sa 3:14
2Pe 2:9
j Yos 23:12
2Nya 15:2
Ezr 8:22
Isa 1:28
Yer 17:13

k Yos 23:16; l Kum 28:20; Isa 63:10; m Kut 19:8; Yos 24:18; Isa 44:5; n Kum 26:17; Mhu 5:4; o Yos 24:15; Zb 119:57; p Kut 20:23; Amu 10:16; 1Sa 7:3; 1Ko 8:5.

Yoshua: "Yehova, Mungu wetu, ndiye tutakayemtumikia, na sauti yake ndiyo tutakayoisikiliza!"[a]

25 Na Yoshua akafanya agano na wale watu siku hiyo na kuwawekea sharti na uamuzi wa hukumu[b] katika Shekemu. **26** Ndipo Yoshua akaandika maneno hayo katika kitabu cha sheria ya Mungu,[c] akachukua jiwe kubwa,[d] akalisimamisha hapo chini ya ule mti mkubwa[e] sana ulio kando ya patakatifu pa Yehova.

27 Naye Yoshua akawaambia watu wote: "Tazameni! Jiwe hili litakuwa ushahidi dhidi yetu,[f] kwa sababu limesikia maneno yote ya Yehova ambayo amesema nasi, nalo litakuwa ushahidi dhidi yenu, ili msije mkamkana Mungu wenu." **28** Basi Yoshua akawaacha watu waende zao, kila mmoja kwenye urithi wake.[g]

29 Na ikawa baada ya mambo hayo, Yoshua mwana wa Nuni mtumishi wa Yehova akafa, akiwa na umri wa miaka mia moja na kumi.[a] **30** Basi wakamzika ndani ya eneo la urithi wake katika Timnath-sera,[b] lililo katika eneo lenye milima la Efraimu, upande wa kaskazini wa Mlima Gaashi. **31** Na Israeli wakaendelea kumtumikia Yehova siku zote za Yoshua na siku zote za wale wanaume wazee walioendelea kuishi baada ya Yoshua,[c] waliokuwa wamejua kazi yote ya Yehova ambayo alifanya kwa ajili ya Israeli.[d]

32 Na kuhusu ile mifupa ya Yosefu,[e] ambayo wana wa Israeli walikuwa wameileta kutoka Misri, waliizika katika Shekemu ndani ya sehemu ya shamba ambalo Yakobo alinunua kutoka kwa wana wa Hamori,[f] baba ya Shekemu, kwa vipande mia moja vya pesa;[g] nalo likawa urithi wa wana wa Yosefu.[h]

33 Eleazari mwana wa Haruni akafa pia.[i] Basi wakamzika katika Kilima cha Finehasi mwana wake,[j] ambacho alikuwa amempa katika eneo lenye milima la Efraimu.

SURA 24

a Kum 5:27
Kum 28:1
b Kut 24:3
c Kum 31:26
d Mwa 31:45
e Mwa 12:6
Mwa 35:4
f Mwa 31:48
g Amu 2:6

Safu ya 2

a Amu 2:8
b Yos 19:50
Amu 2:9
c Amu 2:7
d Kum 11:2
Kum 31:13
e Mwa 50:25
Kut 13:19
Ebr 11:22
f Mdo 7:16
g Mwa 33:19
h Yos 20:7
i Hes 3:4
Hes 20:26
j Kut 6:25
Amu 20:28

WAAMUZI

1 Na ikawa kwamba baada ya kifo[a] cha Yoshua, wana wa Israeli wakamuuliza[b] Yehova, wakisema: "Ni nani kati yetu atakayepanda kwanza kwa Wakanaani ili kupigana nao?" **2** Na Yehova akasema: "Yuda atapanda.[c] Tazama! Hakika nitaitia nchi hiyo mkononi mwake." **3** Ndipo Yuda akamwambia Simeoni ndugu yake: "Panda pamoja nami kuingia katika kura yangu,[d] ili tupate kupigana na Wakaanani, nami nitaenda pamoja nawe katika kura yako."[a] Basi Simeoni akaenda pamoja naye.[b]

4 Kwa hiyo Yuda akaenda, kisha Yehova akawatia Wakanaani na Waperizi mikononi mwao,[c] nao wakawashinda katika Bezeki, watu elfu kumi. **5** Walipomkuta Adoni-bezeki kule Bezeki, ndipo wakapigana naye, wakawashinda Wakanaani[d] na

SURA 1

a Yos 24:29
b Hes 27:21
Amu 20:18
Met 3:5
c Mwa 49:8
Kum 33:7
1Nya 5:2
1Nya 28:4
d Yos 15:1
Yos 19:1

Safu ya 2

a Yos 19:9
b Amu 1:17
c Kum 9:3
Yos 10:8
d Mwa 10:6
Kum 20:17

Waperizi.[a] **6** Wakati Adonibezeki alipoanza kukimbia, wakamfuatilia na kumshika, wakamkata vidole gumba vya mikono yake na vidole vikubwa vya miguu yake. **7** Kwa hiyo Adoni-bezeki akasema: "Kumekuwa na wafalme 70 wakiokota chakula chini ya meza yangu, ambao vidole gumba vya mikono yao na vidole vikubwa vya miguu yao vimekatwa. Mungu amenilipa kulingana na matendo yangu."[b] Baadaye wakamleta Yerusalemu[c] naye akafia huko.

8 Zaidi ya hayo, wana wa Yuda wakaendelea kupigana vita na jiji la Yerusalemu[d] nao wakaliteka, wakalipiga kwa makali ya upanga, kisha wakateketeza jiji hilo kwa moto. **9** Baadaye wana wa Yuda wakashuka kupigana na Wakanaani waliokaa katika eneo lenye milima na Negebu[e] na Shefela.[f] **10** Basi Yuda akapiga mwendo kwenda juu ya Wakanaani waliokuwa wakikaa katika Hebroni[g] (basi jina la Hebroni hapo zamani lilikuwa Kiriath-arba),[h] nao wakamuua Sheshai na Ahimani na Talmai.[i]

11 Na kutoka hapo wakasonga mbele juu ya wakaaji wa Debiri.[j] (Basi jina la Debiri hapo zamani lilikuwa Kiriath-seferi.)[k] **12** Ndipo Kalebu[l] akasema: "Yeyote atakayepiga Kiriath-seferi na kuliteka, nitampa Aksa[m] binti yangu awe mke wake."[n] **13** Naye Othnieli[o] mwana wa Kenasi,[p] ndugu mdogo wa Kalebu,[q] akaliteka. Kwa hiyo yeye akampa Aksa binti yake awe mke wake.[r] **14** Na ikawa kwamba mwanamke huyo alipokuwa akienda nyumbani, akaendelea kumchochea aombe shamba kutoka kwa baba yake. Kisha mwanamke huyo akapiga makofi akiwa juu ya punda.[a] Basi Kalebu akamwambia: "Unataka nini?" **15** Naye akamwambia: "Nipe baraka,[b] kwa maana umenipa sehemu ya shamba upande wa kusini, nawe unipe Guloth-maimu." Basi Kalebu akampa Gulothi ya Juu[c] na Gulothi ya Chini.

16 Na wana wa yule Mkeni,[d] ambaye Musa alikuwa mwanamkwe wake,[e] wakapanda kutoka katika lile jiji la mitende[f] pamoja na wana wa Yuda, wakaingia katika nyika ya Yuda, iliyoko upande wa kusini wa Aradi.[g] Ndipo wakaenda, wakaanza kukaa na watu hao.[h] **17** Lakini Yuda akasonga mbele akiwa na Simeoni ndugu yake, nao wakawapiga Wakanaani waliokaa Sefathi na kuliharibu[i] jiji. Basi jina la jiji hilo likaitwa Horma.[j] **18** Kisha Yuda akateka Gaza[k] na eneo lake na Ashkeloni[l] na eneo lake na Ekroni[m] na eneo lake. **19** Na Yehova akaendelea kuwa na Yuda, naye akamiliki eneo lenye milima, lakini hakuweza kuwafukuza wakaaji wa ile nchi tambarare ya chini, kwa sababu walikuwa na magari ya vita[n] yenye miundu ya chuma.[o] **20** Walipompa Kalebu jiji la Hebroni, kama alivyoahidi Musa,[p] ndipo akawafukuza kutoka humo wale wana watatu wa Anaki.[q]

21 Na wana wa Benyamini hawakuwafukuza Wayebusi waliokaa Yerusalemu;[r] bali Wayebusi wanaendelea kukaa pamoja na wana wa Benyamini katika Yerusalemu mpaka leo.[s]

22 Wakati huohuo nyumba ya Yosefu[t] pia ikapanda kwenda kupigana na Betheli,[u] na Yehova alikuwa pamoja nao.[v] **23** Na

SURA 1

a Mwa 15:20
Kut 3:8
Yos 9:1
Amu 3:5
1Fa 9:20
b Kut 21:23
Law 24:19
Kum 19:21
1Sa 15:33
Ro 2:6
Ga 6:7
c Yos 15:8
d Yos 15:63
Amu 1:21
e Hes 21:1
f Kum 1:7
Yos 11:16
Yos 15:33
g Yos 11:21
Yos 15:13
h Yos 14:15
i Yos 15:14
j Yos 10:38
k Yos 15:15
l Hes 13:6
Hes 14:24
Kum 1:36
Yos 14:13
m 1Nya 2:49
n Yos 15:16
o Yos 15:17
Amu 3:9
p 1Nya 4:13
q Amu 3:9
r 1Sa 17:25

Safu ya 2

a Yos 15:18
b Yos 14:13
Yos 21:12
c Yos 15:19
d Hes 24:21
Amu 4:11
e Kut 3:1
Kut 4:18
Kut 18:1
Hes 10:29
f Kum 34:3
Amu 3:13
2Nya 28:15
g Hes 21:1
h Hes 10:32
i Law 27:29
Kum 20:16
Yos 6:21
j Hes 21:3
Yos 19:4
1Nya 4:30
k Mwa 10:19
Yos 11:22
Yer 25:20
l Yos 13:3
Amu 14:19
Yer 47:5
m Yos 13:3
Yos 15:45
n Kum 20:1
o Yos 17:16
p Hes 14:24
Yos 14:9
q Hes 13:22
r Amu 3:5
s Yos 15:63
2Sa 5:6
t Yos 14:4
Yos 16:1
u Amu 21:19
v Mwa 49:24
Zb 44:3

nyumba ya Yosefu ikaanza kufanya upelelezi[a] juu ya Betheli
(jina la jiji hilo hapo zamani lilikuwa Luzi),[b] **24** na walinzi
wakaona mtu akitoka katika jiji.
Kwa hiyo wakamwambia: "Tafadhali tuonyeshe njia ya kuingia ndani ya jiji, nasi hakika tutakutendea fadhili."[c] **25** Basi
mtu huyo akawaonyesha njia ya kuingia ndani ya jiji; nao wakalipiga jiji kwa makali ya upanga,[d] lakini wakamwachilia mtu huyo
pamoja na familia yake yote.[e] **26** Ndipo mtu huyo akaenda katika nchi ya Wahiti,[f] akajenga jiji na kuliita jina Luzi. Hilo ndilo
jina la jiji hilo mpaka leo.

27 Na Manase[g] hakumiliki Beth-sheani[h] na miji yake ya
kandokando na Taanaki[i] na miji yake ya kandokando na wakaaji
wa Dori[j] na miji yake ya kandokando na wakaaji wa Ibleamu[k]
na miji yake ya kandokando na wakaaji wa Megido[l] na miji yake
ya kandokando, bali Wakanaani waliendelea kukaa katika nchi
hiyo.[m] **28** Na ikawa kwamba Israeli walipopata nguvu,[n] ndipo
wakawatia Wakanaani katika kazi ya kulazimishwa,[o] wala
hawakuwafukuza kabisa.[p]

29 Wala Efraimu hakuwafukuza Wakanaani waliokuwa wakikaa Gezeri, lakini Wakanaani
waliendelea kukaa kati yao katika Gezeri.[q]

30 Zabuloni[r] hakuwafukuza wakaaji wa Kitroni na wakaaji wa Nahaloli,[s] lakini Wakanaani waliendelea kukaa kati yao,[t]
nao wakatiwa katika kazi ya kulazimishwa.[u]

31 Asheri[v] hakuwafukuza wakaaji wa Ako na wakaaji wa
Sidoni[w] na Alabu na Akzibu[x] na Helba na Afiki[y] na Rehobu.[z]
32 Na Waasheri wakaendelea kukaa kati ya Wakanaani waliokaa katika nchi, kwa sababu hawakuwafukuza.[a]

33 Naftali[b] hakuwafukuza wakaaji wa Beth-shemeshi na
wakaaji wa Beth-anathi,[c] lakini waliendelea kukaa kati ya Wakanaani waliokaa katika nchi;[d]
na wakaaji wa Beth-shemeshi na wale wa Beth-anathi wakawatumikia katika kazi ya kulazimishwa.[e]

34 Na Waamori wakaendelea kuwasukuma wana wa Dani[f]
mpaka ndani ya lile eneo lenye milima, kwa maana hawakuwaruhusu washuke kuja chini katika nchi tambarare ya chini.[g]
35 Kwa hiyo Waamori wakaendelea kukaa katika Mlima Heresi na katika Aiyaloni[h] na Shaalbimu.[i] Lakini mkono wa nyumba ya Yosefu ukawa mzito sana hivi kwamba wakalazimishwa kufanya kazi ngumu.[j]
36 Na eneo la Waamori lilikuwa kutoka mpando wa Akrabimu,[k]
kutoka Sela na juu yake.

2 Ndipo malaika[l] wa Yehova akapanda kutoka Gilgali[m]
akaenda Bokimu[n] na kusema: "Mimi niliwatoa ninyi Misri na
kuwaleta katika nchi ambayo niliwaapia mababu zenu.[o] Zaidi ya hayo, nikasema, 'Sitavunja kamwe agano langu pamoja nanyi.[p] **2** Nanyi kwa upande wenu, hampaswi kufanya agano na wakaaji wa nchi
hii.[q] Bomoeni madhabahu zao.'[r] Lakini hamkuisikiliza sauti
yangu.[s] Kwa nini mmefanya hivi?[t] **3** Basi, mimi kwa upande wangu nimesema, 'Sitawafukuza kutoka mbele yenu,
nao watakuwa mitego kwenu,[u] na miungu yao itakuwa mtego
kwenu.'"[v]

SURA 1
a Hes 13:2; Yos 2:1; Yos 7:2
b Mwa 35:6
c Yos 2:14; 1Sa 20:14; 1Sa 30:15
d Yos 8:24
e Yos 6:25; 1Sa 15:6
f Kum 7:1; Yos 9:1
g Yos 17:1
h Yos 17:11
i Yos 21:25; Amu 5:19
j Yos 12:23; Yos 17:12
k 2Fa 9:27; 1Nya 6:70
l 1Fa 9:15; 2Fa 9:27
m Yos 16:10; Yos 17:12; Amu 1:19
n Kum 11:8
o Mwa 9:25; Yos 17:13; 1Fa 9:21
p Hes 33:55; Kum 7:2; Kum 20:16
q Yos 16:10; 1Fa 9:16
r Yos 19:10
s Yos 19:15
t Kum 20:17
u Amu 2:2
v Yos 19:24
w Yos 11:8; Yos 19:28
x Yos 19:29
y Yos 19:30
z Yos 21:31

Safu ya 2
a Zb 106:34; Yer 48:10
b Yos 19:32
c Yos 19:38
d Kum 7:2
e Amu 1:28
f Yos 19:40
g Yos 19:47; Amu 18:1
h Yos 10:12
i Yos 19:42
j Yos 16:10; Yos 17:13
k Hes 34:4; Yos 15:3

SURA 2
l Kut 3:2; Kut 23:20; Kut 23:23; Yos 5:13
m Yos 5:9
n Amu 2:5
o Mwa 12:7; Mwa 26:3
p Mwa 17:7; Law 26:42; Zb 105:8; Mal 3:6; Ebr 6:18
q Kut 23:32; Kum 7:2; 2Ko 6:14
r Kut 34:13; Hes 33:52
s Yos 17:13; Amu 1:19; Amu 1:28; Zb 106:34;
t Kut 23:21;
u Hes 33:55; Yos 23:13;
v Kut 23:33; Kut 34:12; Kum 7:16; 1Fa 11:2; Zb 78:58; Zb 106:36.

4 Na ikawa kwamba mara
tu malaika wa Yehova alipo-
kuwa amewaambia wana wote
wa Israeli maneno hayo, watu
wakaanza kupaaza sauti zao,
wakalia.[a] **5** Kwa hiyo wakaita
jina la mahali pale Bokimu. Ki-
sha wakamtolea Yehova dhabi-
hu hapo.

6 Wakati Yoshua alipowaa-
cha watu waende zao, ndipo
wana wa Israeli wakaenda zao,
kila mmoja kwa urithi wake,
wapate kuimiliki nchi.[b] **7** Na
watu wakaendelea kumtumi-
kia Yehova siku zote za Yoshua
na siku zote za wale wanaume
wazee walioendelea kuishi baa-
da ya Yoshua na ambao waliku-
wa wameona kazi yote kubwa
ya Yehova ambayo aliwafanyia
Israeli.[c] **8** Kisha Yoshua mwa-
na wa Nuni, mtumishi wa Yeho-
va, akafa akiwa na umri wa mia-
ka mia moja na kumi.[d] **9** Basi
wakamzika katika eneo la uri-
thi wake kule Timnath-heresi[e]
katika eneo lenye milima la
Efraimu, upande wa kaskazini
wa Mlima Gaashi.[f] **10** Na kile
kizazi chote pia kikakusanywa
kwa baba zao,[g] na kizazi ki-
ngine kikaanza kutokea baada
yao ambacho hakikumjua Yeho-
va wala ile kazi ambayo alikuwa
amewafanyia Israeli.[h]

11 Na wana wa Israeli wa-
kaanza kufanya yaliyo maba-
ya machoni pa Yehova,[i] wa-
katumikia Mabaali.[j] **12** Hivyo
wakamwacha Yehova Mungu
wa baba zao aliyekuwa amewa-
toa katika nchi ya Misri,[k] wa-
kafuata miungu mingine kuto-
ka kati ya miungu ya watu wali-
owazunguka pande zote,[l] waka-
anza kuiinamia, hata wakamtia
uchungu Yehova.[m] **13** Hivyo
wakamwacha Yehova, wakaa-
nza kutumikia Baali na sanamu
za Ashtorethi.[a] **14** Ndipo ha-
sira ya Yehova ikawaka juu
ya Israeli,[b] akawatia mikono-
ni mwa waporaji, nao wakaa-
nza kuwapora;[c] naye akawau-
za mkononi mwa adui zao wali-
owazunguka pande zote,[d] wala
hawakuweza tena kusimama
mbele ya adui zao.[e] **15** Koko-
te walikoenda, mkono wa Yeho-
va ulikuwa juu yao ili kuwa-
letea msiba,[f] kama vile Yehova
alivyokuwa amesema na kama
vile Yehova alivyokuwa ame-
waapia;[g] nao wakawa katika
dhiki kali sana.[h] **16** Basi Ye-
hova alikuwa akisimamisha wa-
amuzi,[i] nao walikuwa wakiwao-
koa kutoka mkononi mwa wa-
poraji wao.[j]

17 Nao hawakuwasikiliza
hata waamuzi wao, lakini waka-
fanya uasherati[k] na miungu
mingine[l] na kuiinamia. Wa-
ligeuka upesi kutoka katika
njia ambayo mababu zao wa-
likuwa wametembea kwa ku-
tii amri za Yehova.[m] Wao ha-
wakufanya hivyo. **18** Na wa-
kati Yehova alipowasimamishia
waamuzi,[n] Yehova akawa pamo-
ja na mwamuzi huyo, naye aka-
waokoa kutoka mkononi mwa
adui zao siku zote za mwamu-
zi huyo; kwa maana Yehova ali-
kuwa akijuta[o] kwa ajili ya kuu-
gua kwao kwa sababu ya waka-
ndamizaji[p] wao na wale waliko-
kuwa wakiwasukuma huku na
huku.

19 Na ikawa kwamba mwa-
muzi huyo alipokufa, waliku-
wa wakigeuka na kutenda kwa
njia ya uharibifu hata zaidi ya
baba zao kwa kufuata miungu
mingine ili kuitumikia na kuiin-
amia.[q] Hawakujiepusha na ma-
tendo yao na tabia yao ya ukai-
di.[r] **20** Mwishowe hasira ya Ye-
hova ikawaka[s] juu ya Israeli

SURA 2

a 1Sa 7:6
b Yos 24:28
c Yos 23:3
Yos 24:31
d Yos 24:29
e Yos 19:50
f Yos 24:30
g Amu 2:7
Mhu 1:4
h Kum 6:12
Kum 31:13
Amu 2:17
1Nya 28:9
i Amu 6:1
2Nya 33:2
j Amu 3:7
Amu 10:6
1Fa 18:18
2Nya 28:2
Yer 2:23
Ho 2:13
k Kum 13:5
Kum 28:15
Kum 31:16
l Kum 6:14
Amu 10:6
m Kut 20:5
Kum 7:4

Safu ya 2

a Amu 3:7
Amu 10:6
1Sa 7:3
1Fa 11:5
2Fa 23:13
Zb 106:36
b Amu 3:8
2Nya 36:16
Zb 106:40
c Law 26:17
2Fa 17:20
Zb 106:41
d Amu 4:2
Zb 44:12
Isa 50:1
e Law 26:37
Kum 28:25
f Kum 28:15
Yer 21:10
g Kum 4:25
Kum 4:26
Kum 7:4
h Kum 4:30
Amu 10:9
i Amu 3:9
1Sa 12:11
j Ne 9:27
Zb 106:43
k Zb 73:27
Yer 3:8
Yer 3:14
Eze 23:3
Eze 23:30
Yak 4:4
l Kut 34:15
Law 17:7
m Kut 32:8
Kum 9:12
Amu 2:7
n Amu 3:9
o Kum 32:36
Zb 90:13
Zb 106:45
p Kut 2:24
Amu 4:3
2Fa 13:4
q Amu 4:1
Amu 8:33
r Zb 78:8
Isa 48:4
s Kut 32:10
Kum 7:4
Kum 32:22
Amu 10:7
Zb 106:40

naye akasema: "Kwa sababu taifa hili wamevunja agano[a] langu ambalo niliwaamuru mababu zao, nao hawakuisikiliza sauti yangu,[b] **21** mimi pia, kwa upande wangu, sitafukuza tena kutoka mbele yao hata taifa moja kati ya yale mataifa ambayo Yoshua aliacha wakati alipokufa,[c] **22** ili kwa njia ya hayo Israeli wajaribiwe,[d] kuona kama wataishika njia ya Yehova kwa kutembea katika hiyo kama vile mababu zao walivyoishika, au hapana." **23** Kwa hiyo Yehova akayaacha mataifa hayo yabaki kwa kutoyafukuza upesi,[e] wala hakuyatia mkononi mwa Yoshua.

3 Basi haya ndiyo mataifa[f] ambayo Yehova aliacha yabaki ili kupitia hayo ajaribu[g] Israeli, yaani, wale wote ambao hawakuona vita vyovyote vya Kanaani;[h] **2** kusudi kwamba vizazi vya wana wa Israeli vipate kufunzwa, ili kuwafundisha vita, yaani, wale tu ambao hawakuwa wameona mambo kama hayo kabla ya wakati ule: **3** Wakuu watano wa muungano[i] wa Wafilisti,[j] na Wakanaani[k] wote, pia Wasidoni[l] na Wahivi[m] waliokaa katika Mlima Lebanoni[n] kutoka Mlima Baal-hermoni[o] mpaka maingilio ya Hamathi.[p] **4** Nao wakaendelea kutumika kama vyombo vya kujaribu[q] Israeli ili kujua kama wangetii amri za Yehova ambazo alikuwa ameamuru baba zao kupitia Musa.[r] **5** Na wana wa Israeli wakakaa katikati ya Wakanaani,[s] Wahiti na Waamori na Waperizi na Wahivi na Wayebusi.[t] **6** Nao wakaanza kuoa binti zao,[u] na binti zao wenyewe wakawapa wana wao,[v] nao wakaanza kuitumikia miungu yao.[w]

SURA 2

a Kut 24:3
Kut 24:8
Kut 34:27
Kum 29:1
Yos 23:16
b Law 26:14
Kum 28:15
Zb 106:34
c Yos 13:2
d Hes 33:55
Kum 8:2
Yos 23:13
Amu 3:4
Met 17:3
e Kut 23:30
Kum 7:22

SURA 3

f Kut 23:30
g Kum 8:2
2Nya 32:31
h Amu 2:10
i Yos 13:3
1Sa 6:18
j Mwa 21:32
Amu 1:19
k Mwa 10:15
l Yos 13:4
Amu 1:31
m Mwa 10:17
Kut 3:17
Yos 9:1
n Kum 1:7
Yos 13:6
o Kum 3:9
Yos 13:5
p Hes 34:8
q Kut 23:33
Hes 33:55
r Amu 2:22
s Amu 1:29
Zb 106:34
t Kut 3:8
Kut 3:17
Kum 7:1
Yos 9:1
u Kut 34:16
v Kum 7:3
Ezr 9:12
w Hes 25:2
1Fa 11:4

Safu ya 2

a Amu 2:11
b Kum 31:16
Amu 10:6
c Kut 34:13
Kum 12:3
Kum 16:21
1Fa 16:33
d Amu 2:20
e Law 26:17
Amu 2:14
1Sa 12:9
f Mwa 24:10
g Kum 4:30
Amu 2:18
Amu 3:15
Zb 107:19
h Amu 2:16
i Yos 15:17
j 1Nya 4:13
k Amu 1:13
l Hes 11:17
Amu 6:34
Amu 11:29
Amu 14:6
Amu 15:14
1Sa 11:6
1Sa 16:13
2Nya 15:1
Isa 63:11
m Zek 4:6
Ebr 11:33

7 Basi wana wa Israeli wakafanya yaliyokuwa mabaya machoni pa Yehova, wakamsahau Yehova Mungu wao,[a] wakatumikia Mabaali[b] na miti mitakatifu.[c] **8** Ndipo hasira ya Yehova ikawaka juu ya Israeli,[d] naye akawauza[e] mkononi mwa Kushan-rishathaimu mfalme wa Mesopotamia;[f] na wana wa Israeli wakaendelea kumtumikia Kushan-rishathaimu kwa miaka minane. **9** Na wana wa Israeli wakaanza kumwita Yehova awape msaada.[g] Ndipo Yehova akasimamisha mwokozi[h] kwa ajili ya wana wa Israeli ili apate kuwaokoa, Othnieli[i] mwana wa Kenasi,[j] ndugu mdogo wa Kalebu.[k] **10** Basi roho[l] ya Yehova ikaja juu yake, naye akawa mwamuzi wa Israeli. Alipoenda vitani, Yehova akamtia Kushan-rishathaimu mfalme wa Siria mkononi mwake na mkono wake ukamshinda nguvu[m] Kushan-rishathaimu. **11** Baada ya hapo nchi haikuwa na usumbufu wowote kwa miaka 40. Mwishowe Othnieli mwana wa Kenasi akafa.

12 Kisha wana wa Israeli wakaanza tena kufanya yaliyo mabaya machoni pa Yehova.[n] Ndipo Yehova akaacha Egloni mfalme wa Moabu[o] apate nguvu juu ya Israeli,[p] kwa sababu walifanya yaliyo mabaya machoni pa Yehova.[q] **13** Zaidi ya hayo, akakusanya wana wa Amoni[r] na Amaleki[s] juu yao. Ndipo wakaenda, wakapiga Israeli na kulichukua jiji la mitende.[t] **14** Na wana wa Israeli wakaendelea kumtumikia Egloni mfalme wa Moabu kwa miaka kumi na minane.[u] **15** Na wana wa Isra-

n Amu 2:19; Ho 6:4; **o** Mwa 19:37; **p** Amu 2:14; Yoh 19:11; **q** Law 26:14; **r** Mwa 19:38; Amu 11:4; **s** Kut 17:8; Amu 6:3; Zb 83:7; **t** Kum 34:3; Amu 1:16; 2Nya 28:15; **u** Law 26:25; Kum 28:48.

eli wakaanza kumwita Yehova awape msaada.[a] Basi Yehova akawasimamishia mwokozi, Ehudi[b] mwana wa Gera Mbenyamini,[c] mwanamume mwenye kutumia mkono wa kushoto.[d] Baada ya muda wana wa Israeli wakapeleka ushuru kupitia mkono wake kwa Egloni mfalme wa Moabu. **16** Wakati huohuo Ehudi akajifanyia upanga, nao ulikuwa na makali kuwili,[e] urefu wake ukiwa mkono mmoja. Kisha akaufunga chini ya vazi lake kwenye paja[f] lake la kuume. **17** Naye akampa Egloni mfalme wa Moabu[g] ushuru huo. Basi Egloni alikuwa ni mtu mnene sana.

18 Na ikawa kwamba alipokuwa amemaliza kutoa ule ushuru,[h] mara moja akawaambia watu waende zao, wale waliobeba ule ushuru. **19** Naye mwenyewe akageuka na kurudi alipofika mahali penye machimbo yaliyokuwa katika Gilgali,[i] akasema: "Nina neno la siri kwako, Ee mfalme." Basi akasema: "Nyamazeni!" Ndipo wote waliokuwa wamesimama kando yake wakatoka nje na kumwacha.[j] **20** Na Ehudi akamjia alipokuwa ameketi katika chumba chake cha darini chenye baridi ambacho kilikuwa chake binafsi. Naye Ehudi akaendelea kusema: "Nina neno linalotoka kwa Mungu kwa ajili yako." Kwa hiyo akasimama kutoka katika kiti chake cha ufalme. **21** Ndipo Ehudi akatia ndani mkono wake wa kushoto, akauchukua ule upanga kutoka kwenye paja lake la kuume na kuuingiza ndani ya tumbo lake. **22** Nao mpini pia ukazidi kuingia ndani ukiufuata upanga huo na mafuta yakaufunika upanga huo, kwa maana hakuuchomoa upanga kutoka katika tumbo lake, na mavi yakaanza kutoka nje. **23** Naye Ehudi akatoka nje kupitia tundu la hewa, lakini akaifunga kwa ufunguo milango ya chumba cha dari. **24** Naye akatoka nje.[a]

Na watumishi wa mfalme wakaja na kuanza kuangalia, na tazama, milango ya chumba cha dari ilikuwa imefungwa kwa ufunguo. Kwa hiyo wakasema: "Ameenda haja[b] katika chumba chake cha ndani chenye baridi." **25** Nao wakaendelea kungojea mpaka wakaona aibu, na, tazama! hakuna aliyeifungua milango ya kile chumba cha dari. Ndipo wakachukua ufunguo na kuifungua, na, tazama! bwana wao alikuwa ameanguka chini, naye amekufa!

26 Lakini Ehudi alikimbia walipokuwa bado wanakawia, naye akapita kando ya yale machimbo ya mawe,[c] akakimbia, akaenda Seira. **27** Na ikawa kwamba alipofika huko akaanza kupiga baragumu[d] katika eneo lenye milima la Efraimu;[e] na wana wa Israeli wakaanza kushuka pamoja naye kutoka katika eneo lenye milima, yeye akiwa mbele yao. **28** Ndipo akawaambia: "Nifuateni,[f] kwa maana Yehova amewatia adui zenu, Wamoabu, mkononi mwenu."[g] Nao wakamfuata, wakateka vivuko[h] vya Yordani juu ya Wamoabu, wala hawakumruhusu mtu yeyote avuke. **29** Na wakati huo wakapiga Moabu, karibu wanaume elfu kumi,[i] kila mmoja akiwa ni mwenye nguvu[j] na kila mmoja akiwa ni mwanamume shujaa; wala hakuna hata mtu mmoja aliyepona.[k] **30** Na Moabu wakatiishwa siku hiyo chini ya mkono wa Israeli;

SURA 3

a Amu 3:9
Zb 50:15
Zb 78:34
Zb 107:13
Yer 29:12

b Amu 4:1

c Mwa 49:27

d Amu 20:16
1Nya 12:2

e Zb 149:6

f Zb 45:3

g Amu 11:18

h 2Fa 23:35

i Yos 4:19
Yos 5:9

j Met 14:15

Safu ya 2

a Mhu 10:10

b 1Sa 24:3
1Fa 18:27

c Amu 3:19

d Yos 6:5
Amu 6:34
1Sa 13:3
2Sa 2:28
Yoe 2:1

e Yos 16:5
Amu 7:24

f Amu 2:16

g Amu 7:15
1Sa 17:47

h Yos 2:7
Amu 12:5

i Law 26:8
Kum 28:7

j Amu 3:17
Zb 17:10

k Law 26:7

na nchi haikuwa na usumbufu
wowote tena kwa miaka 80.[a]
31 Na baada yake kukawa na
Shamgari[b] mwana wa Anathi,
naye akawapiga Wafilisti,[c] wa-
naume mia sita, kwa mchokoo
wa ng'ombe; naye pia akawao-
koa Israeli.[d]

4 Ndipo wana wa Israeli wa-
kaanza tena kufanya yali-
yokuwa mabaya machoni pa Ye-
hova kwa vile sasa Ehudi aliku-
wa amekufa.[e] **2** Basi Yehova
akawauza[f] mkononi mwa Yabi-
ni mfalme wa Kanaani, aliyeta-
wala katika Hasori;[g] na mkuu
wa jeshi lake alikuwa ni Sisera,[h]
naye alikuwa anakaa Haroshe-
thi[i] ya mataifa. **3** Na wana wa
Israeli wakaanza kumlilia Yeho-
va,[j] kwa sababu Yabini alikuwa
na magari 900 ya vita yenye mi-
undu ya chuma,[k] naye kwa miaka
20 akawakandamiza wana
wa Israeli[l] kwa ukali.
4 Basi Debora, nabii wa
kike,[m] mke wa Lapidothi, ndi-
ye aliyekuwa akihukumu Israe-
li wakati huo. **5** Naye alikuwa
anakaa chini ya mtende wa De-
bora kati ya Rama[n] na Bethe-
li[o] katika eneo lenye milima
la Efraimu; na wana wa Israe-
li wakawa wakimwendea ili awa-
hukumu. **6** Naye akatuma uju-
mbe kumwita Baraka[p] mwana
wa Abinoamu kutoka Kedesh-
naftali,[q] akamwambia: "Je, Ye-
hova Mungu wa Israeli haku-
toa amri? 'Nenda, usambae kati-
ka Mlima Tabori,[r] nawe uchukue
wanaume elfu kumi kutoka kwa
wana wa Naftali[s] na kutoka kwa
wana wa Zabuloni.[t] **7** Nami
hakika nitamvuta kwako[u] Sise-
ra[v] mkuu wa jeshi la Yabini[w] na
magari yake ya vita na umati
wake, kwenye bonde la mto la
Kishoni,[x] nami hakika nitamtia
yeye mkononi mwako.'"[y]

SURA 3

a Law 26:6
Amu 3:11
b Amu 5:6
c Kut 23:31
Yos 13:2
Amu 15:3
d Amu 15:15
1Sa 13:19
1Sa 13:22
1Sa 17:47
1Sa 17:50

SURA 4

e Amu 2:19
f Law 26:17
Kum 28:25
Kum 32:30
Amu 2:14
Amu 3:8
Amu 10:7
g Yos 19:36
h 1Sa 12:9
i Amu 4:16
j Amu 2:18
Amu 3:9
Zb 107:19
Zb 145:19
k Kum 20:1
Yos 17:16
Amu 1:19
l Kum 28:48
Zb 106:42
m Kut 15:20
2Fa 22:14
Lu 2:36
Mdo 21:9
1Ko 11:5
n Yos 18:25
Amu 19:13
1Fa 15:17
Yer 40:1
o Mwa 28:17
Mwa 28:19
Yer 48:13
Amo 3:14
p Ebr 11:32
q Yos 21:32
r Zb 89:12
Yer 46:18
s Mwa 30:8
Mwa 35:25
Yos 19:32
t Mwa 30:20
Mwa 35:23
Yos 19:10
u Kut 14:4
v 1Sa 12:9
w Amu 4:2
x 1Fa 18:40
Zb 83:9
y Kum 20:1

Safu ya 2

a Amu 5:24
Amu 5:26
Amu 9:54
b Yos 20:7
Yos 21:32
Amu 4:6
c Amu 5:18
d Amu 4:6
e Amu 1:16
f Mwa 15:19
Hes 24:21
1Sa 15:6
g Hes 10:29
h Amu 5:12
i Amu 4:6
j Kum 20:1
Amu 4:3
k Amu 4:7
Amu 5:21
Zb 83:9

8 Ndipo Baraka akamwa-
mbia: "Ukienda pamoja nami,
mimi pia nitaenda; lakini usipo-
enda pamoja nami, mimi sita-
enda." **9** Basi yule nabii aka-
sema: "Hakika nitaenda pa-
moja nawe. Hata hivyo, kile
kitu cha kurembesha hakita-
kuwa chako katika njia unayo-
iendea, kwa kuwa Yehova ata-
muuza Sisera katika mkono
wa mwanamke."[a] Ndipo Debo-
ra akasimama, akaenda pamo-
ja na Baraka mpaka Kedeshi.[b]
10 Na Baraka akaanza kuita
Zabuloni[c] na Naftali waje Ke-
deshi, nao wakapanda wanau-
me elfu kumi wakifuata hatua
zake;[d] na Debora akapanda pa-
moja naye.
11 Lakini Heberi[e] Mkeni aliku-
wa amejitenga na Wake-
ni,[f] wana wa Hobabu, amba-
ye Musa alikuwa mwana-mkwe
wake,[g] naye alikuwa amelisi-
mamisha hema lake karibu na
ule mti mkubwa kule Saananim-
mu, ambao uko katika Kedeshi.
12 Ndipo wakampasha Sise-
ra habari kwamba Bara-
ka mwana wa Abinoamu[h] ame-
panda kwenda Mlima Tabori.[i]
13 Mara moja Sisera akakusa-
nya pamoja magari yake yote
ya vita, yale magari mia tisa ya
vita yenye miundu ya chuma,[j]
na watu wote waliokuwa pamo-
ja naye, kutoka Haroshethi ya
mataifa mpaka kwenye bonde
la mto la Kishoni.[k] **14** Ndipo
Debora akamwambia Baraka:
"Simama, kwa maana hii ndi-
yo siku ambayo Yehova hakika
atamtia Sisera mkononi mwa-
ko. Je, Yehova siye ambaye ame-
enda mbele yako?"[l] Na Baraka
akashuka kutoka Mlima Tabo-
ri akiwa na wanaume elfu kumi

l Kum 9:3; Ro 8:31.

nyuma yake. **15** Ndipo Yehova akaanza kumvuruga[a] Sisera na magari yake yote ya vita na kambi yote kwa makali ya upanga mbele ya Baraka. Mwishowe Sisera akashuka kutoka garini, akaanza kukimbia kwa miguu. **16** Kisha Baraka akafuatilia[b] yale magari ya vita[c] na ile kambi mpaka Haroshethi ya mataifa, hivi kwamba kambi yote ya Sisera ikaanguka kwa makali ya upanga. Hakubaki hata mmoja.[d]

17 Lakini Sisera[e] akakimbia kwa miguu mpaka kwenye hema la Yaeli[f] mke wa Heberi Mkeni,[g] kwa maana kulikuwa na amani kati ya Yabini mfalme wa Hasori[h] na nyumba ya Heberi Mkeni. **18** Ndipo Yaeli akatoka nje kumpokea Sisera, akamwambia: "Karibia huku, bwana wangu, karibia huku kwangu. Usiogope." Basi akakaribia kwake, akaingia katika hema. Baadaye akamfunika kwa blangeti. **19** Kisha akamwambia: "Tafadhali, nipe maji kidogo ya kunywa, kwa maana nina kiu." Basi huyo mwanamke akafungua kiriba[i] cha maziwa, akampa kinywaji,[j] kisha akamfunika. **20** Naye akamwambia tena: "Simama mlangoni pa hema, na itakuwa kwamba yeyote akija na kukuuliza na kusema, 'Je, yupo mwanamume yeyote hapa?' ndipo useme, 'Hapana!'"

21 Na Yaeli mke wa Heberi akachukua kigingi cha hema, akashika nyundo mkononi mwake. Kisha akaenda kwake kimyakimya, akakipigilia kile kigingi katika kipaji cha uso wake,[k] akakipigilia mpaka kikaingia katika udongo, huyo akiwa amelala usingizi mzito na kuchoka. Basi akafa.[l]

SURA 4

a Kut 14:24
Yos 10:10
2Fa 7:6
b Law 26:7
Yos 10:19
c Isa 43:17
d Kum 7:23
e Amu 4:2
1Sa 12:9
f Amu 5:6
Amu 5:24
g Hes 24:21
Amu 1:16
Amu 4:11
h Amu 4:2
i Mwa 21:19
j Amu 5:25
k Amu 5:26
l Amu 4:9
Amu 5:27

Safu ya 2

a 1Nya 22:18
Ne 9:24
Zb 18:47
Zb 47:3
Zb 81:14
Ebr 11:33
b Mwa 9:25
Kum 28:13
c Law 26:7
Kum 7:24

SURA 5

d Amu 4:4
e Ebr 11:32
f Amu 4:6
g Kut 15:1
Kum 31:19
Kum 31:30
1Nya 16:9
Zb 18:Uta
h Amu 4:10
Zb 110:3
i Kut 18:10
2Nya 20:26
Zb 145:2
j Zb 119:46
k 2Sa 22:50
Zb 7:17
l Kut 5:1
Kut 20:2
m Kum 33:2
Zb 68:7
n Hab 3:3
o 2Sa 22:8
p Zb 68:8
q Kum 4:11
Zb 97:5
r Ne 9:13
s Kut 19:18
t Kut 5:1
Kut 20:2

22 Na, tazama! Baraka alikuwa anamfuatilia Sisera. Basi Yaeli akatoka nje kumpokea, akamwambia: "Njoo, nami nitakuonyesha mtu unayemtafuta." Basi akaingia kwake ndani, na, tazama! Sisera alikuwa ameanguka na amekufa, nacho kigingi kikiwa katika kipaji cha uso wake.

23 Kwa hiyo Mungu akamtiisha[a] Yabini mfalme wa Kanaani mbele ya wana wa Israeli siku hiyo. **24** Na mkono wa wana wa Israeli ukaendelea kuwa mgumu zaidi na zaidi juu ya Yabini mfalme wa Kanaani,[b] mpaka walipokuwa wamemkatilia mbali Yabini mfalme[c] wa Kanaani.

5 Na katika siku hiyo Debora[d] pamoja na Baraka[e] mwana wa Abinoamu[f] wakaanza kuimba,[g] wakisema:

2 "Kwa kuacha nywele
zining'inie katika Israeli
kwa ajili ya vita,
Kwa ajili ya watu kujitolea,[h]
Mbarikini Yehova.[i]
3 Sikilizeni, enyi wafalme;[j]
tegeni sikio, enyi maofisa
wakuu:
Ndiyo, nitamwimbia
Yehova.
Nitampigia muziki[k]
Yehova, Mungu wa
Israeli.[l]
4 Yehova, ulipotoka Seiri,[m]
Ulipopiga mwendo kutoka
shamba la Edomu,[n]
Dunia ilitikisika,[o] mbingu
pia zikatiririka maji,[p]
Mawingu pia yakatiririka
maji.
5 Milima ikayeyuka kutoka
mbele za uso wa Yehova,[q]
Mlima Sinai[r] kutoka mbele
za uso wa Yehova,[s] Mungu
wa Israeli.[t]

6 Katika siku za Shamgari[a]
mwana wa Anathi,
Katika siku za Yaeli,[b] njia
hazikuwa na wapitaji,
Na wasafiri wa barabarani
wakawa wakisafiri kwa
njia za kuzunguka.[c]
7 Wakaaji katika nchi
iliyo wazi wakakoma,
wakakoma katika
Israeli,[d]
Mpaka mimi, Debora,[e]
niliposimama,
Mpaka niliposimama kama
mama katika Israeli.[f]
8 Wakaanza kuchagua
miungu mipya.[g]
Ndipo kukawa na vita
malangoni.[h]
Ngao haikuonekana, wala
mkuki,
Kati ya 40,000 katika
Israeli.[i]
9 Moyo wangu uko pamoja na
viongozi wa Israeli,[j]
Waliojitolea kati ya watu.[k]
Mbarikini Yehova.[l]
10 Enyi wapandaji wa
punda-jike[m] wenye rangi
nyekundu ya kimanjano,
Enyi mnaokaa kwenye
mazulia yenye thamani,
Nanyi mnaotembea
barabarani,
Angalieni![n]
11 Sauti za wenye kugawa maji
katika mahali pa kuteka
maji,[o]
Hapo walianza kusimulia
matendo ya uadilifu ya
Yehova,[p]
Matendo ya uadilifu ya
wakaaji wake katika nchi
iliyo wazi katika Israeli.
Ndipo watu wa Yehova
walipoondoka na kwenda
mpaka malangoni.
12 Amka, amka, ewe Debora;[q]
Amka, amka, imba wimbo![r]
Simama, Baraka,[a]
wachukue mateka wako,
ewe mwana wa
Abinoamu![b]
13 Ndipo wenye kuokoka
wakashuka kwenda kwa
walio mashuhuri;
Watu wa Yehova walishuka
kuja kwangu ili kupigana
na wanaume wenye
nguvu.
14 Asili yao ilikuwa katika
Efraimu katika nchi
tambarare ya chini,[c]
Pamoja nawe, Ee
Benyamini, kati ya watu
wako.
Kutoka Makiri[d] viongozi
walishuka,
Na kutoka Zabuloni wale
wanaotumia vifaa vya
mwandishi.[e]
15 Na wakuu katika Isakari[f]
walikuwa pamoja na
Debora,
Na kama Isakari, ndivyo
alivyokuwa Baraka.[g]
Alipelekwa kwa miguu
katika nchi tambarare ya
chini.[h]
Katikati ya migawanyo
ya Rubeni kulikuwa na
uchunguzi mkubwa wa
moyo.[i]
16 Kwa nini uliketi kati ya
yale mafumba mawili ya
matandiko,
Ili kusikiliza zumari
zikipigiwa makundi?[j]
Kulikuwa na uchunguzi
mkubwa wa moyo[k] kwa
ajili ya migawanyo ya
Rubeni.
17 Gileadi alijikalia katika
makao yake ng'ambo ile
nyingine ya Yordani;[l]
Na Dani, kwa nini
aliendelea kukaa wakati
huo katika meli?[m]

SURA 5

a Amu 3:31
b Amu 4:17
c Law 26:22
Isa 33:8
d Amu 4:2
e Amu 4:4
f Amu 4:5
g Kum 32:16
Amu 2:12
Amu 4:1
h Hes 33:56
Amu 4:2
i Amu 4:3
1Sa 13:19
j Amu 4:6
k Amu 4:10
Zb 110:3
l Amu 5:2
Zb 103:1
m Amu 10:4
Amu 12:14
n Zb 105:2
Zb 145:5
o Kut 2:16
p Kum 32:4
1Sa 12:7
Zb 145:7
Mik 6:5
q Amu 4:4
r Amu 5:1

Safu ya 2

a Amu 4:6
b Amu 5:1
c Yos 16:4
d Hes 32:39
e 2Fa 25:19
2Nya 26:11
f Mwa 49:15
1Nya 12:32
g Amu 4:6
Ebr 11:32
h Amu 4:14
i Met 3:27
j Hes 32:1
Hes 32:24
k Yak 4:17
l Yos 22:9
m Yos 19:46
Yon 1:3

Asheri aliketi kizembe
kando ya bahari,
Akaendelea kukaa mahali
pake pa kushukia pwani.[a]
18 Zabuloni ni watu
waliodharau nafsi zao
karibu kufa;[b]
Naftali[c] pia, kwenye vilele
vya shamba.[d]
19 Wafalme walikuja,
wakapiga vita;
Ndipo wafalme wa Kanaani
wakapiga vita[e]
Katika Taanaki[f] kando ya
maji ya Megido.[g]
Hawakuchukua faida
yoyote ya fedha.[h]
20 Nyota zilipigana zikiwa
mbinguni,[i]
Zikiwa kwenye mizunguko
yao zilipigana na Sisera.
21 Mto wa Kishoni
ukawafagilia mbali,[j]
Mto wa siku za kale, mto
wa Kishoni.[k]
Wewe ulikanyagia chini
nguvu,[l] ewe nafsi yangu.
22 Ndipo kwato za farasi
zikakanyaga-kanyaga[m]
Kwa sababu ya
kutimuka-timuka kwa
farasi-dume zake.
23 ‘Laani[n] Merozi,’ akasema
malaika wa Yehova,[o]
‘Walaani wakaaji wake bila
kukoma,
Kwa sababu hawakuja
kumsaidia Yehova,
Kumsaidia Yehova pamoja
na wanaume wenye
nguvu.’
24 Yaeli[p] mke wa Heberi
Mkeni,[q] atabarikiwa zaidi
kati ya wanawake,
Kati ya wanawake katika
mahema atabarikiwa
zaidi.[r]
25 Aliomba maji, akampa
maziwa;

SURA 5
a Yos 19:24
b Amu 4:10
Amu 6:35
1Nya 12:33
Zb 68:27
c Amu 4:6
d Amu 4:14
e Kum 7:24
Amu 4:13
f Amu 1:27
g Yos 12:21
h Amu 4:16
Amu 5:30
i Mwa 18:14
Yos 10:11
Amu 4:15
1Sa 7:10
Zb 135:7
j Amu 4:7
Zb 83:9
k Amu 4:13
Zb 44:3
l Zb 44:5
Isa 25:10
Mik 7:10
m Zb 20:7
Zb 147:10
Met 21:31
Isa 5:28
n Yer 48:10
o Kut 23:23
Amu 2:1
p Amu 4:17
q Hes 24:21
Amu 1:16
Amu 4:11
r Met 31:31

Safu ya 2
a Amu 4:19
b Met 31:17
c Amu 4:21
d Amu 4:22
e Met 7:6
Wim 2:9
f Amu 4:15
1Sa 15:33
g Amu 4:16
h 2Sa 14:2
2Sa 20:16
i Kut 15:9
j Kum 20:14
Kum 21:11

Alimpa maziwa ya mgando[a]
katika bakuli kubwa la
karamu la walio
mashuhuri.
26 Akanyoosha mkono wake
akashika kigingi cha
hema,
Nao mkono wake wa
kuume ukashika nyundo
ya mti ya wafanyakazi
wenye bidii.[b]
Akampiga Sisera kwa
nyundo hiyo, akatoboa
kichwa chake,[c]
Akapasua na kukata kipaji
cha uso wake.
27 Aliporomoka katikati ya
miguu yake, alianguka,
akalala chini;
Aliporomoka katikati ya
miguu yake, alianguka;
Hapo alipoporomoka,
ndipo alipoanguka akiwa
ameshindwa.[d]
28 Mwanamke alichungulia
nje dirishani, akaendelea
kumngojea,
Mama ya Sisera akiwa
kwenye dirisha lenye
matundu,[e]
‘Kwa nini gari lake la vita
limechelewa kuja?[f]
Kwa nini vishindo vya
kwato za magari yake
vichelewe sana hivyo?’[g]
29 Wenye hekima kati ya
bibi[h] zake wenye vyeo
walikuwa wakimjibu,
Ndiyo, yeye pia alikuwa
akijibu kwa maneno yake
mwenyewe,
30 ‘Je, haiwapasi wao
kupata, haiwapasi wao
kugawanya nyara,[i]
Tumbo moja la
uzazi—matumbo mawili
ya uzazi kwa kila
mwanamume,[j]

Nyara za vitu vilivyotiwa
rangi kwa ajili ya Sisera,
nyara za vitu vilivyotiwa
rangi,
Vazi lililopambwa, vitu
vilivyotiwa rangi, mavazi
mawili yaliyopambwa
Kwa ajili ya shingo za
wanaume wa nyara?'
31 Na waangamie hivyo adui
zako wote,[a] Ee Yehova,
Na wanaokupenda[b] wawe
kama wakati jua
linaposonga katika
nguvu zake."[c]
Na nchi ikawa bila usumbufu
tena kwa miaka 40.[d]

6 Ndipo wana wa Israeli wakaanza kufanya yaliyokuwa mabaya machoni pa Yehova.[e] Basi Yehova akawatia mkononi mwa Midiani[f] kwa miaka saba. **2** Nao mkono wa Midiani ukawa na nguvu juu ya Israeli.[g] Kwa sababu ya Midiani, wana wa Israeli walijifanyia maghala ya chini ya udongo yaliyokuwa katika milima, na mapango na mahali palipo pagumu kufikiwa.[h] **3** Na ikatukia kwamba, Israeli wakipanda mbegu,[i] Midiani na Amaleki[j] na watu wa Mashariki[k] walikuwa wakija, ndiyo, walikuja kupigana nao. **4** Nao wakawa wakipiga kambi juu yao na kuyaharibu mazao ya nchi mpaka Gaza, na hawakuruhusu mazao yoyote wala kondoo wala ng'ombe wala punda kubaki katika Israeli.[l] **5** Kwa maana wao pamoja na mifugo yao walikuwa wakija na mahema yao. Walikuja wakiwa wengi kama nzige,[m] na wao pamoja na ngamia zao hawakuwa na hesabu;[n] nao walikuwa wakiingia katika nchi ili kuiharibu.[o] **6** Na Israeli wakawa maskini sana kwa sababu ya Midiani; nao wana wa Israeli wakaanza kumwomba Yehova msaada.[a]

7 Na ikawa kwamba kwa kuwa wana wa Israeli walimwomba Yehova msaada kwa sababu ya Midiani,[b] **8** Yehova akamtuma mwanamume mmoja, nabii,[c] kwa wana wa Israeli, akawaambia: "Yehova Mungu wa Israeli amesema hivi, 'Mimi ndiye niliyewaleta ninyi mpande kutoka Misri,[d] nikawatoa katika nyumba ya watumwa.[e] **9** Kwa hiyo nikawakomboa ninyi kutoka katika mkono wa Misri na kutoka katika mkono wa wakandamizaji wenu wote, nikawafukuza kutoka mbele yenu, nikawapa ninyi nchi yao.[f] **10** Zaidi ya hayo, nikawaambia ninyi: "Mimi ni Yehova Mungu wenu.[g] Msiogope miungu ya Waamori[h] ambao mnakaa katika nchi yao."[i] Nanyi hamkuisikiliza sauti yangu.'"[j]

11 Baadaye malaika wa Yehova akaja[k] na kuketi chini ya mti mkubwa uliokuwa katika Ofra, mali yake Yoashi Mwabiezeri,[l] wakati Gideoni[m] mwana wake alipokuwa akipepeta ngano katika shinikizo la divai ili kuiondoa haraka machoni pa Midiani. **12** Ndipo malaika wa Yehova akamtokea, akamwambia: "Yehova yupo pamoja nawe,[n] Ee mwanamume shujaa na mwenye nguvu." **13** Kwa hiyo Gideoni akamwambia: "Nakuomba radhi, bwana wangu, lakini ikiwa Yehova yupo pamoja nasi, kwa nini haya yote yametupata,[o] na yako wapi matendo yake yote ya ajabu[p] ambayo mababu zetu walitusimulia,[q] wakisema, 'Je, Yehova siye aliyetuleta kutoka Misri?'[r] Na sasa Yehova ame-

SURA 5
a Zb 68:2; Zb 83:9; Zb 92:9
b Kut 20:6; Zb 91:14; Zb 97:10; Ro 8:28; 1Ko 8:3
c Zb 110:3; Da 12:3; Mt 13:43
d Law 26:6; Amu 3:11; Amu 3:30

SURA 6
e Kum 28:15; Amu 2:19; Ne 9:28
f Mwa 25:2; Law 26:17; Hes 25:17; Kum 28:48; Amu 2:14
g Law 26:21; Hes 33:55; Kum 28:51
h 1Sa 13:6
i Law 26:16; Kum 28:33
j Amu 3:13
k Mwa 29:1; Amu 8:10; 1Fa 4:30
l Kum 28:31; Kum 28:48; Mik 6:15
m Amu 8:10
n Amu 7:12
o Zb 83:4

Safu ya 2
a Kum 4:30; Zb 50:15
b Amu 2:18; Zb 86:7; Zb 107:19; Ho 5:15
c Hes 12:6; Amo 3:7
d Kut 20:2; Law 26:13
e Amu 2:1; Zb 78:52; Zb 136:11
f Kum 7:2; Yos 10:42; Ne 9:24; Zb 44:2; Zb 78:55
g Kum 6:4; Zb 81:10; Ho 13:4
h 2Fa 17:35; Yer 10:2
i Yos 24:15
j Kum 28:15; Amu 2:2; Yer 3:13; Sef 3:2
k Amu 2:1
l Yos 17:2; Amu 6:24; Amu 8:32
m Mwa 49:24; Ebr 11:32
n Yos 1:5; Amu 2:18
o Amu 6:2
p Isa 63:15
q Kum 4:9; Kum 6:7; Zb 44:1; Zb 78:3
r Kut 13:14

tuacha,[a] naye anatutia katika
mkono wa Midiani." **14** Ndipo
Yehova akamtazama na kusema: "Nenda katika nguvu zako
hizi,[b] nawe hakika utawaokoa
Israeli kutoka katika mkono
wa Midiani.[c] Je, si mimi ni-
nayekutuma?"[d] **15** Yeye naye
akamwambia: "Nakuomba ra-
dhi, Yehova. Nitawaokoa Israe-
li na nini?[e] Tazama! Elfu ya-
ngu ndiyo ndogo zaidi katika
Manase, na mimi ndiye mdo-
go zaidi katika nyumba ya
baba yangu."[f] **16** Lakini Yeho-
va akamwambia: "Kwa sababu
nitakuwa pamoja nawe,[g] nawe
hakika utapiga Midiani[h] kama
mtu mmoja."

17 Ndipo akamwambia: "Iki-
wa sasa nimepata kibali macho-
ni pako,[i] unifanyie ishara kwa-
mba wewe ndiwe unayesema
nami.[j] **18** Tafadhali, usiondo-
ke hapa mpaka nije kwako[k] na
kukuletea zawadi yangu na ku-
iweka mbele yako."[l] Basi aka-
sema: "Mimi nitaendelea kuke-
ti hapa mpaka utakaporudi."
19 Na Gideoni akaingia nda-
ni, akatayarisha mwana-mbuzi[m]
na efa ya unga kuwa keki zi-
sizo na chachu.[n] Akaweka nya-
ma katika kikapu, mchuzi aka-
uweka katika chungu cha kupi-
kia, kisha akamletea hapo nje
chini ya ule mti mkubwa, akavi-
pakua.

20 Basi yule malaika wa Mu-
ngu wa kweli akamwambia:
"Chukua nyama hiyo na keki
hizo zisizo na chachu, uviwe-
ke juu ya lile jiwe kubwa pale,[o]
ukaumimine huu mchuzi." Aka-
fanya hivyo. **21** Ndipo malai-
ka wa Yehova akainyoosha ncha
ya fimbo iliyokuwa mkononi
mwake, akaigusa ile nyama na
zile keki zisizo na chachu, na
moto ukaanza kupanda kutoka

SURA 6

a Kum 31:17
2Nya 15:2
b Mwa 49:24
c Amu 6:32
Amu 8:22
1Sa 12:11
Ebr 11:32
d Yos 1:9
Amu 4:6
Ro 8:31
e Zb 44:3
f 1Sa 9:21
Lu 14:11
Flp 2:3
g Kum 3:22
Kum 20:4
Amu 2:18
Isa 41:10
h Law 26:8
Zb 83:9
i Kut 33:13
j Kut 3:12
k Mwa 18:3
Mwa 19:3
Amu 13:15
l Mwa 18:5
Amu 6:19
m Mwa 18:7
n Mwa 18:6
o Amu 13:19

Safu ya 2

a Law 9:24
Amu 13:20
1Fa 18:38
1Nya 21:26
2Nya 7:1
b Amu 13:8
Amu 13:9
Amu 13:21
Ebr 13:2
c Mwa 16:7
Mwa 16:13
Mwa 32:24
Mwa 32:30
Amu 13:22
Lu 1:12
d Lu 24:36
e Da 10:19
f Mwa 32:30
g Amu 13:20
h Mwa 22:14
Kut 17:15
i Amu 8:32
Amu 9:5
j Kut 23:24
Kum 12:3
k Kut 34:13
Kum 7:5
1Ko 8:4
l Kum 12:1
m Mt 10:16

katika ule mwamba, ukaiketeke-
teza ile nyama na zile keki zisi-
zo na chachu.[a] Na yule malaika
wa Yehova akatoweka macho-
ni pake. **22** Kwa hiyo Gideoni
akatambua kwamba alikuwa ni
malaika wa Yehova.[b]

Mara moja Gideoni akasema:
"Ole wangu, Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova, kwa sababu
nimeona malaika wa Yehova uso
kwa uso!"[c] **23** Lakini Yehova
akamwambia: "Amani iwe pa-
moja nawe.[d] Usiogope.[e] Hutaku-
fa."[f] **24** Basi Gideoni akamje-
ngea Yehova madhabahu[g] hapo,
nayo inaendelea kuitwa[h] jina
Yehova-shalomu mpaka leo hii.
Bado iko katika Ofra[i] ya Waa-
biezeri.

25 Na ikawa usiku huo kwa-
mba Yehova akamwambia tena:
"Mchukue yule ng'ombe-dume
mchanga, yule ng'ombe-dume
wa baba yako, yaani, yule
ng'ombe-dume mchanga wa pili
mwenye miaka saba, nawe ubo-
moe madhabahu ya Baali[j] amba-
yo ni ya baba yako, na ule mti
mtakatifu ulio kando yake, uu-
kate.[k] **26** Nawe umjengee Ye-
hova Mungu wako madhabahu
mbele ya ngome hii, kwa mi-
stari ya mawe, nawe umchu-
kue ng'ombe-dume mchanga
wa pili, umtoe kama toleo la
kuteketezwa juu ya kuni za
ule mti mtakatifu ambao utau-
kata." **27** Basi Gideoni aka-
wachukua wanaume kumi
kati ya watumishi wake, aka-
fanya kama vile Yehova alivyo-
kuwa amemwambia;[l] lakini ika-
wa kwamba, kwa kuwa aliogo-
pa mno nyumba ya baba yake
na watu wa jiji, hakuweza kuya-
fanya hayo mchana, aliyafanya
usiku.[m]

28 Watu wa jiji walipoamka
asubuhi na mapema kama

kawaida, tazama! madhabahu
ya Baali ilikuwa imebomolewa
na ule mti mtakatifu[a] uliokuwa
kando yake ulikuwa umekatwa,
na yule ng'ombe-dume mcha-
nga wa pili alikuwa ametolewa
juu ya madhabahu ambayo ili-
kuwa imejengwa. **29** Nao wa-
kaanza kusemezana: "Ni nani
ambaye amefanya jambo hili?"
Wakauliza-uliza na kutafuta.
Mwishowe wakasema: "Gideoni
mwana wa Yoashi ndiye aliyefa-
nya jambo hili." **30** Kwa hiyo
watu wa jiji wakamwambia Yo-
ashi: "Mtoe nje mwana wako
afe,[b] kwa sababu amebomoa ma-
dhabahu ya Baali, na kwa saba-
bu amekata mti mtakatifu uli-
okuwa kando yake." **31** Ndi-
po Yoashi[c] akawaambia wote
waliosimama kumpinga:[d] "Je,
ninyi ndio mtakaomtetea ki-
sheria Baali ili kuona kama
ninyi wenyewe mnaweza ku-
mwokoa? Yeyote atakayemte-
tea kisheria anapaswa kuuawa
asubuhi hii.[e] Ikiwa yeye ni Mu-
ngu,[f] acheni ajitetee mwenye-
we kisheria,[g] kwa sababu
mtu fulani amebomoa madha-
bahu yake." **32** Naye akaanza
kumwita jina Yerubaali[h] siku
hiyo, akisema: "Baali na ajite-
tee mwenyewe kisheria, kwa
sababu mtu fulani amebomoa
madhabahu yake."[i]
33 Na Midiani[j] wote na Amale-
ki[k] na watu wa Mashariki[l] wa-
kakusanyika kama mtu mmo-
ja,[m] wakavuka na kupiga kambi
katika nchi tambarare ya chini
ya Yezreeli.[n] **34** Na roho ya Ye-
hova[o] ikamfunika Gideoni naye
akaanza kupiga baragumu,[p] na
Waabiezeri[q] wakakusanywa pa-
moja kumfuata. **35** Naye aka-
tuma wajumbe[r] katika Manase
yote, nao pia wakakusanywa pa-
moja kumfuata. Pia akatuma
wajumbe kotekote katika Ashe-
ri na Zabuloni na Naftali, nao
wakaja kukutana naye.
36 Ndipo Gideoni akamwa-
mbia Mungu wa kweli: "Ikiwa
utawaokoa Israeli kupitia
kwangu, kama vile ambavyo
umeahidi,[a] **37** tazama, nina-
weka manyoya ya kondoo yaki-
wa wazi katika uwanja wa ku-
puria. Umande ukija juu ya
manyoya hayo peke yake laki-
ni nchi yote hapo iwe kavu, ndi-
po nitakapojua kwamba utawa-
okoa Israeli kupitia kwangu,
kama vile ambavyo umeahidi."
38 Na ikawa hivyo. Alipoamka
mapema siku iliyofuata na ku-
kamua manyoya hayo, akatoa
katika manyoya hayo umande
wa kutosha kujaza maji bakuli
kubwa la karamu. **39** Hata hi-
vyo, Gideoni akamwambia Mu-
ngu wa kweli: "Usiache hasi-
ra yako iwake juu yangu, bali
acha niseme tena mara moja
tu. Tafadhali, acha nifanye ja-
ribio mara moja tu kwa manyo-
ya hayo. Tafadhali, acha ukavu
uje juu ya manyoya hayo peke
yake, na umande uje juu ya nchi
yote." **40** Basi Mungu akafa-
nya hivyo usiku huo; na uka-
vu ukaja kuwa juu ya manyo-
ya peke yake, na umande ukawa
juu ya nchi yote.

7 Ndipo Yerubaali,[b] yaani, Gi-
deoni,[c] na watu wote walioki-
kuwa pamoja naye, wakaondo-
ka mapema na kupiga kambi
kando ya kisima cha Harodi;
na kambi ya Midiani ilikuwa
upande wake wa kaskazi-
ni, kwenye kilima cha More,
katika nchi tambarare ya chini.
2 Sasa Yehova akamwambia
Gideoni: "Watu ulio nao ni we-
ngi mno nisiweze kuwatia Mi-
diani mkononi mwao.[d] Labda
Israeli watajivuna[e] dhidi ya-

SURA 6
a Kum 12:3
2Fa 18:4
2Nya 31:1
b Yer 26:11
Yoh 16:2
c Amu 6:11
d Kut 23:2
Amu 6:28
e Kum 13:5
Kum 17:3
Kum 17:5
f Kut 15:11
Zb 115:5
Da 2:47
1Ko 8:5
g 1Fa 18:26
1Fa 18:39
Isa 41:23
Yer 10:5
1Ko 8:4
h 1Sa 12:11
2Sa 11:21
i 1Fa 18:27
j Mwa 25:2
Hes 25:17
Amu 6:2
k Mwa 36:12
Kut 17:16
Hes 24:20
Kum 25:19
l Mwa 29:1
Amu 6:3
m Amu 7:12
n Yos 17:16
Yos 19:18
o Amu 3:10
Amu 11:29
Amu 13:25
Amu 14:6
Amu 15:14
Isa 63:11
Zek 4:6
p Amu 3:27
Sef 1:16
q Yos 17:2
Amu 8:2
r Amu 11:12
2Nya 30:6

Safu ya 2
a Amu 6:14

SURA 7
b Amu 6:32
1Sa 12:11
c Amu 6:11
d 1Sa 14:6
2Nya 14:11
e Isa 2:11

ngu, wakisema, 'Mkono wangu
ndio ulioniokoa.'[a] **3** Na sasa
tafadhali, ita masikioni mwa
watu, ukisema, 'Ni nani anaye-
ogopa na kutetemeka? Na aji-
ondoe.'"[b] Basi Gideoni akawa-
fanyia majaribio. Ndipo watu
22,000 wakajiondoa, wakabaki
watu 10,000.

4 Lakini Yehova akamwa-
mbia Gideoni: "Bado kuna watu
wengi mno.[c] Washushe kwenye
maji ili niwajaribu kwa ajili yako
pale. Na itatukia kwamba yeyo-
te nitakayekuambia, 'Huyu ata-
enda pamoja nawe,' yeye ndiye
atakayeenda pamoja nawe, la-
kini yeyote ambaye nitakua-
mbia, 'Huyu hataenda pamoja
nawe,' yeye hataenda." **5** Basi
akawashusha watu majini.[d]

Ndipo Yehova akamwambia
Gideoni: "Kila mtu ambaye ata-
ramba maji kwa ulimi wake
kama vile mbwa anavyoramba,
utamweka kando peke yake,
pia kila mtu atakayepiga mago-
ti yake anapokunywa."[e] **6** Na
hesabu ya wale walioramba kwa
mkono wao wakiuleta kinywa-
ni ikawa watu mia tatu. Lakini
wale watu wengine wote wali-
piga magoti yao walipokunywa
maji.

7 Yehova akamwambia Gide-
oni: "Kwa watu hawa mia tatu
walioramba nitawaokoa ninyi,
nami nitatia Midiani mkononi
mwako.[f] Lakini hawa watu we-
ngine wote na waende kila mmo-
ja mahali pake." **8** Kwa hiyo
wakachukua vyakula vya watu
hao mkononi mwao, na bara-
gumu[g] zao, na watu wote wa
Israeli akawaacha waende zao
kila mmoja nyumbani kwake;
akabaki na wale watu mia tatu.
Nayo kambi ya Midiani ilikuwa
chini yake katika nchi tamba-
rare ya chini.[h]

SURA 7

a 1Sa 17:47
Zb 44:7
Isa 10:13
1Ko 1:29
2Ko 4:7

b Kum 20:8

c 2Nya 32:8
Zb 33:16

d Zb 7:9

e 1Pe 5:8

f Amu 7:2
1Sa 14:6
Isa 41:14
Ebr 11:34

g Yos 6:4
Amu 3:27

h Amu 6:33

Safu ya 2

a Ayu 4:13
Ayu 33:15

b Kum 7:2
Amu 3:10
Amu 4:14
2Nya 16:8
2Nya 20:17

c 2Ko 13:5

d Amu 7:13

e 1Sa 23:16
Ezr 6:22
Ne 6:9
Isa 35:3

f Amu 6:33

g Yer 46:23

h Amu 6:5

i Mt 2:12

j Amu 6:16

k Hes 23:5

l Amu 6:11
Amu 6:14

m Isa 42:8

n Amu 7:7

o Mwa 40:8
Amu 7:11

p Kut 4:31
2Nya 20:18
Zb 95:6

q Amu 4:14

9 Na ikawa kwamba usiku[a]
huo Yehova akamwambia hivi:
"Simama, shuka juu ya kambi
hiyo, kwa maana nimeitia mko-
noni mwako.[b] **10** Lakini iki-
wa unaogopa kushuka, shuka,
wewe pamoja na Pura mtumi-
shi wako, kambini.[c] **11** Nawe
usikilize yale watakayosema,[d]
na baada ya hayo mikono yako
itapata nguvu,[e] nawe hakika
utashuka juu ya kambi hiyo."
Ndipo yeye na Pura mtumishi
wake wakashuka mpaka kwe-
nye ukingo wa wale waliokuwa
wamejipanga kivita, waliokuwa
katika kambi.

12 Sasa Midiani na Amaleki
na watu wote wa Mashariki[f] wa-
likuwa wamejazana katika ile
nchi tambarare ya chini, we-
ngi sana kama nzige;[g] na nga-
mia[h] zao hawakuwa na hesabu,
walikuwa wengi sana kama che-
mbe za mchanga ulio kando ya
bahari. **13** Basi Gideoni aka-
ja, na, tazama! kulikuwa na
mtu akimsimulia mwenzake
ndoto, naye akasema: "Hii ni
ndoto ambayo nimeota.[i] Na, ta-
zama! kulikuwa na keki ya mvi-
ringo ya mkate wa shayiri iki-
geuka-geuka katika kambi ya
Midiani. Ndipo ikaja kwenye
hema na kulipiga nalo likaa-
nguka,[j] ikalipindua juu chini,
na hema hilo likaanguka chini."
14 Naye mwenzake akajibu[k] na
kusema: "Hiki si kitu kingine
bali ni upanga wa Gideoni[l] mwa-
na wa Yoashi, mtu wa Israeli.
Mungu wa kweli[m] ametia Midi-
ani na kambi yote katika mko-
no wake."[n]

15 Na ikawa kwamba, mara
tu Gideoni aliposikia masimu-
lizi ya ndoto hiyo na maele-
zo yake,[o] akaanza kuabudu.[p] Ki-
sha akarudi katika kambi ya
Israeli na kusema: "Simameni,[q]

kwa kuwa Yehova ametia kambi ya Midiani katika mkono wenu.” **16** Ndipo akagawanya wale watu mia tatu katika vikosi vitatu na kuwapa wote mkononi baragumu[a] na mitungi mikubwa mitupu, na mienge ndani ya mitungi hiyo mikubwa. **17** Naye akawaambia: “Jifunzeni kwa kunitazama, nanyi fanyeni vivyo hivyo. Nitakapofika kwenye ukingo wa kambi, iwe kwamba vile nitakavyofanya, fanyeni vivyo hivyo. **18** Nitakapokuwa nimekwisha kupiga baragumu, mimi na wote walio pamoja nami, ninyi pia zipigeni baragumu, kuizunguka kambi yote,[b] nanyi mseme, ‘Upanga wa Yehova[c] na wa Gideoni!’”

19 Baadaye Gideoni akaja na wale wanaume mia moja waliokuwa pamoja naye kwenye ukingo wa kambi mwanzoni mwa kesha la katikati ya usiku.[d] Walikuwa wamemaliza tu kuweka askari-walinzi. Nao wakaanza kuzipiga zile baragumu,[e] na ile mitungi mikubwa ya maji iliyokuwa mikononi mwao ikavunjwa vipande-vipande.[f] **20** Ndipo vile vikosi vitatu vikapiga baragumu[g] na kuivunjavunja ile mitungi mikubwa na kuchukua tena ile mienge kwa mkono wao wa kushoto na zile baragumu katika mkono wao wa kuume ili kuzipiga, nao wakaanza kupaaza sauti: “Upanga wa Yehova[h] na wa Gideoni!” **21** Nao wakaendelea kusimama kila mmoja mahali pake kuzunguka kambi pande zote, na kambi yote ikaanza kupiga mbio, wakapiga kelele na kukimbia.[i] **22** Na wale mia tatu[j] wakaendelea kupiga baragumu,[k] na Yehova akatia upanga wa kila mmoja juu ya mwenzake katika kambi yote;[a] na kambi ikaendelea kukimbia hadi Beth-shita, hadi Serera, hadi kwenye mipaka ya Abel-mehola[b] kando ya Tabathi.

23 Wakati huohuo watu wa Israeli wakakusanywa pamoja kutoka Naftali[c] na Asheri[d] na Manase[e] wote, nao wakawafuatilia[f] Midiani. **24** Na Gideoni akatuma wajumbe katika eneo lote lenye milima la Efraimu,[g] akisema: “Shukeni mkutane na Midiani na mshike hayo maji mbele yao mpaka Beth-bara na Yordani.” Basi watu wote wa Efraimu wakakusanywa pamoja, nao wakayashika maji[h] mpaka Beth-bara na Yordani. **25** Pia wakawakamata wale wakuu wawili wa Midiani, yaani, Orebu na Zeebu;[i] wakamuua Orebu[j] juu ya mwamba wa Orebu, nao wakamuua Zeebu kwenye mtungi wa divai wa Zeebu. Nao wakaendelea kufuatilia Midiani,[k] wakamletea Gideoni kichwa cha Orebu na kile cha Zeebu katika eneo la Yordani.[l]

8 Ndipo watu wa Efraimu wakamwambia: “Umetutendea jambo gani hili kwa kukosa kutuita ulipotoka kwenda kupigana na Midiani?”[m] Nao wakatafuta kwa ukali kugombana naye.[n] **2** Mwishowe akawaambia: “Basi mimi nimefanya nini kwa kulinganishwa nanyi?[o] Je, masalio ya Efraimu[p] si bora kuliko ukusanyaji wa zabibu wa Abiezeri?[q] **3** Mungu aliwatia hao wakuu wa Midiani, Orebu na Zeebu[r] katika mkono wenu, nami nimeweza kufanya nini kwa kulinganishwa nanyi?” Ndipo roho yao ikatulia kumwelekea aliposema neno hilo.[s]

4 Mwishowe Gideoni akaja Yordani, akauvuka, yeye pamoja na wale wanaume mia tatu

SURA 7

a Amu 7:8
Met 20:18
b Amu 7:20
c 1Sa 17:47
2Nya 20:17
d Zb 63:6
Lu 12:38
e Amu 7:8
f Amu 7:16
g Yos 6:4
Amu 7:18
h Kut 14:13
2Nya 20:17
i Kut 14:25
Kum 28:7
2Fa 7:7
j Yos 7:4
Amu 7:6
k Yos 6:6
Amu 7:8
Amu 7:16

Safu ya 2

a 1Sa 14:20
2Nya 20:23
Isa 19:2
Eze 38:21
Zek 14:13
b 1Fa 4:12
1Fa 19:16
c Yos 19:32
Amu 6:35
d Yos 19:24
e Yos 17:1
f 1Sa 14:22
g Amu 3:27
h Amu 3:28
i Amu 8:3
Zb 83:11
j Isa 10:26
k Amu 8:4
l 1Sa 17:54

SURA 8

m Amu 7:2
Met 8:13
Met 16:18
n Amu 12:1
2Sa 19:41
2Nya 25:10
o Met 15:28
Flp 2:3
2Ti 2:24
p Amu 7:25
Met 11:2
q Amu 6:11
Amu 6:34
r Amu 7:25
Zb 83:11
s Met 14:29
Met 15:1
Met 25:15
Mhu 10:4
Ga 5:23

waliokuwa pamoja naye, wa-
kiwa wamechoka lakini wa-
kiwa wanaendelea kufuatilia.
5 Baadaye akawaambia watu
wa Sukothi:[a] "Tafadhali wape-
ni mikate ya mviringo watu
wanaofuata hatua zangu,[b] kwa
kuwa wamechoka nami ninawa-
fuatilia Zeba[c] na Zalmuna,[d] wa-
falme wa Midiani." **6** Lakini
wakuu wa Sukothi wakasema:
"Je, viganja vya mikono ya Zeba
na Zalmuna tayari vimo mko-
noni mwako ili jeshi lako lipe-
we mkate?"[e] **7** Ndipo Gideoni
akasema: "Ndiyo sababu Yehova
atakapowatia Zeba na Zalmuna
katika mkono wangu, hakika
nitaipepeta miili yenu kwa miiba
ya nyikani na michongoma."[f]
8 Naye akatoka hapo na kwe-
nda Penueli,[g] akasema nao vi-
vyo hivyo, lakini watu wa Penu-
eli wakamjibu kama vile watu
wa Sukothi walivyokuwa wa-
memjibu. **9** Basi akawaambia
pia watu wa Penueli: "Nitaka-
porudi kwa amani, nitaubo-
moa mnara huu."[h]

10 Basi Zeba na Zalmuna[i]
walikuwa katika Karkori, nao
walikuwa pamoja na kambi zao,
kukiwa na karibu watu 15,000
waliobaki kutoka katika ka-
mbi nzima ya watu wa Masha-
riki;[j] na wale waliokuwa taya-
ri wameanguka ni watu 120,000
waliokuwa wakitumia upanga.[k]
11 Na Gideoni akaendelea ku-
panda kupitia njia ya wale wa-
naokaa katika mahema upande
wa mashariki wa Noba na Yo-
gbeha,[l] naye akaanza kuisha-
mbulia kambi wakati kambi
hiyo ilipokuwa haijihadhari.[m]
12 Wakati Zeba na Zalmuna
walipoanza kukimbia, akaanza
kuwafuatilia mara moja, aka-
wakamata hao wafalme wawi-
li wa Midiani, Zeba na Zalmu-
na;[a] naye akaitetemesha kambi
nzima.

13 Ndipo Gideoni mwana wa
Yoashi akaanza kurudi kutoka
vitani kupitia ile njia nyemba-
mba inayopanda kwenda Here-
si. **14** Akiwa njiani, akamka-
mata kijana kutoka kwa watu
wa Sukothi[b] na kutafuta habari
kutoka kwake.[c] Basi akamwa-
ndikia majina ya wakuu[d] wa Su-
kothi na wanaume wazee wake,
watu 77. **15** Ndipo akaenda
kwa watu wa Sukothi na kuse-
ma: "Tazameni, Zeba na Zalmu-
na ambao mlinidhihaki kuwa-
husu, mkisema, 'Je, viganja vya
mikono vya Zeba na Zalmuna
tayari vimo mkononi mwako ili
watu wako waliochoka wape-
we mkate?'"[e] **16** Ndipo aka-
wachukua hao wanaume wa-
zee wa jiji na miiba ya nyika-
ni na michongoma, naye akaitu-
mia kuwafundisha somo watu
wa Sukothi.[f] **17** Naye akabo-
moa mnara[g] wa Penueli,[h] kisha
akawaua watu wa jiji hilo.

18 Kisha akawaambia Zeba
na Zalmuna:[i] "Wale watu mli-
owaua katika Tabori[j] walikuwa
watu wa namna gani?" Wakase-
ma: "Kama wewe ulivyo, ndivyo
wao walivyokuwa, kila mmoja
wao, kama wana wa mfalme ka-
tika umbo." **19** Kwa hiyo aka-
sema: "Hao walikuwa ndugu
zangu, wana wa mama yangu.
Kama Yehova anavyoishi, iki-
wa mngeliwahifadhi hai, si-
ngeliwaua ninyi."[k] **20** Ndipo
akamwambia Yetheri mzaliwa
wake wa kwanza: "Simama,
waue." Lakini huyo kijana ha-
kuchomoa upanga wake, kwa
sababu aliogopa, kwa maana
bado alikuwa kijana tu.[l]
21 Basi Zeba na Zalmuna waka-
sema: "Simama wewe mwenye-
we utushambulie, kwa maana

SURA 8

a Mwa 33:17
Yos 13:27
Zb 108:7
b 1Sa 25:8
2Sa 17:28
c Amu 8:21
d Zb 83:11
e Kum 23:4
Amu 5:23
1Sa 25:10
1Sa 25:11
Met 3:27
Yak 2:16
f Amu 8:16
Ga 6:7
g Mwa 32:31
1Fa 12:25
h Amu 8:17
i Amu 8:5
Zb 83:11
j Amu 7:12
Ebr 11:34
k Kum 28:7
l Hes 32:35
m Amu 18:27
Met 20:18

Safu ya 2

a Zb 83:11
b Amu 8:5
c Amu 1:24
1Sa 30:15
d Amu 8:6
e Amu 8:6
Met 3:27
f Amu 8:7
Met 10:13
Met 19:29
g Amu 8:9
h Mwa 32:31
Amu 8:8
1Fa 12:25
i Zb 83:11
j Zb 89:12
k Mwa 9:6
Hes 35:19
l 1Sa 17:33

jinsi mwanamume alivyo, ndivyo zilivyo nguvu zake."[a] Kwa hiyo Gideoni akasimama na kuwaua[b] Zeba na Zalmuna, naye akachukua yale mapambo yenye umbo la mwezi yaliyokuwa katika shingo za ngamia zao.

22 Baadaye watu wa Israeli wakamwambia Gideoni: "Tawala juu yetu,[c] wewe na mwana wako na mjukuu wako vilevile, kwa maana umetuokoa kutoka katika mkono wa Midiani."[d] **23** Lakini Gideoni akawaambia: "Mimi mwenyewe sitatawala juu yenu, wala mwanangu hatatawala juu yenu.[e] Yehova ndiye atakayetawala juu yenu."[f] **24** Kisha Gideoni akawaambia tena: "Acheni niwaombe jambo moja: Kila mmoja wenu anipe pete ya pua[g] ya nyara yake." (Kwa maana walikuwa na pete za pua za dhahabu, kwa sababu walikuwa Waishmaeli.)[h] **25** Ndipo wakasema: "Hakika tutazitoa." Basi wakatandika nguo ya kujitanda, na kila mmoja wao akatupa ndani yake pete ya pua ya nyara yake. **26** Na uzito wa zile pete za pua za dhahabu ambazo alikuwa ameomba ukajumlika kuwa shekeli elfu moja na mia saba za dhahabu, mbali na yale mapambo yenye umbo la mwezi[i] na herini na mavazi ya sufu iliyotiwa rangi ya zambarau[j] ambayo wale wafalme wa Midiani walikuwa wamevaa, na pia mbali na ile mikufu iliyokuwa katika shingo za ngamia.[k]

27 Naye Gideoni akavifanya kuwa efodi[l] na kuiweka katika jiji lake la Ofra[m] ili ionekane; na Israeli wote wakaanza kufanya uasherati nayo hapo,[n] nayo ikawa mtego kwa Gideoni na kwa nyumba yake.[o]

SURA 8

a Amu 6:12
b 1Sa 15:33
Zb 83:11
c Kum 17:14
Amu 9:8
1Sa 8:6
1Sa 12:12
Ho 13:10
d Amu 6:14
e 2Sa 22:26
Met 2:8
f Kut 15:18
1Sa 10:19
Zb 10:16
Zb 29:10
Zb 146:10
Isa 33:22
Isa 43:15
Da 4:3
g Mwa 24:22
h Mwa 16:11
Mwa 25:13
Mwa 28:9
Mwa 37:28
i Amu 8:21
Isa 3:18
j Est 8:15
Yer 10:9
Eze 27:7
k Amu 8:21
l Kut 28:6
Amu 17:5
Amu 18:14
m Amu 6:11
n Kut 23:33
Amu 2:17
Zb 106:39
Ho 4:12
o Amu 8:33

Safu ya 2

a Amu 6:1
Zb 83:9
b Law 26:6
Amu 3:11
Amu 5:31
c Amu 6:32
1Sa 12:11
d Amu 9:2
e Amu 9:1
2Sa 11:21
f Amu 6:11
Amu 6:24
g Amu 2:17
Amu 2:19
Amu 10:6
h Amu 9:4
i Amu 3:7
Zb 106:36
j Zb 106:43
k Mwa 40:23
Met 3:27
l Amu 9:16
Mhu 9:15
2Ti 3:2

SURA 9

m Amu 8:31
2Sa 11:21
n Mwa 12:6
Mwa 33:18
Mwa 34:27
1Fa 12:1
Mdo 7:16
o Amu 8:30

28 Hivyo Midiani[a] wakatiishwa mbele ya wana wa Israeli, nao hawakuinua kichwa chao tena; na nchi haikuwa na usumbufu wowote tena kwa miaka 40 katika siku za Gideoni.[b]

29 Na Yerubaali[c] mwana wa Yoashi akaenda zake, akaendelea kukaa katika nyumba yake.

30 Naye Gideoni akaja kuwa na wana 70[d] waliotoka katika viuno vyake, kwa maana alikuja kuwa na wake wengi. **31** Na yule suria wake aliyekuwa katika Shekemu, yeye pia akamzalia mwana. Basi akamwita jina lake Abimeleki.[e] **32** Mwishowe Gideoni mwana wa Yoashi akafa akiwa mwenye umri mwema wa uzeeni, akazikwa katika kaburi la Yoashi baba yake katika Ofra la Waabiezeri.[f]

33 Na ikawa kwamba mara tu Gideoni alipokufa, wana wa Israeli wakaanza tena kufanya uasherati na Mabaali,[g] nao wakamfanya Baal-berithi kuwa mungu wao.[h] **34** Na wana wa Israeli hawakumkumbuka Yehova Mungu wao,[i] aliyewakomboa kutoka katika mkono wa adui zao wote pande zote;[j] **35** nao hawakuonyesha fadhili zenye upendo[k] kwa nyumba ya Yerubaali, Gideoni, kwa kuufuata wema wote ambao aliwaonyesha Israeli.[l]

9 Baada ya muda Abimeleki[m] mwana wa Yerubaali akaenda Shekemu[n] kwa ndugu za mama yake, akaanza kusema nao na kusema na familia yote ya nyumba ya baba ya mama yake, akisema: **2** "Tafadhali, semeni masikioni mwa wenye mashamba wote wa Shekemu, 'Ni jambo gani lililo bora kwenu, kwamba watu 70,[o] wana wote wa Yerubaali, watawale

juu yenu au mtu mmoja atawale juu yenu? Nanyi mkumbuke kwamba mimi ni mfupa na nyama yenu.'"[a]

3 Basi ndugu za mama yake wakaanza kusema maneno hayo yote kumhusu yeye masikioni mwa wenye mashamba wote wa Shekemu, na mioyo yao ikaelekea kwa Abimeleki,[b] kwa maana walisema: "Yeye ni ndugu yetu."[c] **4** Ndipo wakampa vipande 70 vya fedha kutoka katika nyumba ya Baal-berithi,[d] kisha Abimeleki akavitumia kukodisha watu wazembe na wenye dharau,[e] ili wafuatane naye. **5** Kisha akaenda nyumbani kwa baba yake katika Ofra,[f] akawaua ndugu zake,[g] wana wa Yerubaali, watu 70, juu ya jiwe moja, lakini Yothamu mwana mdogo zaidi wa Yerubaali akaachwa, kwa sababu alijificha.

6 Baadaye, watu wote wenye mashamba wa Shekemu na nyumba yote ya Milo[h] wakakusanyika pamoja wakaenda, wakamfanya Abimeleki atawale akiwa mfalme,[i] karibu na ule mti mkubwa,[j] nguzo iliyokuwa katika Shekemu.[k]

7 Wakati walipompasha Yothamu habari, akaenda mara moja, akasimama juu ya kilele cha Mlima Gerizimu,[l] akapaaza sauti yake, akaita na kuwaambia: "Nisikilizeni, enyi wenye mashamba wa Shekemu, na acheni Mungu awasikilize ninyi:

8 "Hapo zamani za kale, miti ilienda kumtia mafuta mfalme juu yao. Basi ikauambia mzeituni,[m] 'Uwe mfalme juu yetu.'[n] **9** Lakini mzeituni ukaiambia, 'Je, niyaache mafuta yangu ambayo kwayo wao humtukuza[o] Mungu na wanadamu, na je, niende kuwayawaya juu ya miti mingine?'[p] **10** Ndipo miti ikauambia mtini,[a] 'Wewe njoo, uwe malkia juu yetu.' **11** Lakini mtini ukaiambia, 'Je, niache utamu wangu na mazao yangu mema, na je, niende kuwayawaya juu ya miti mingine?'[b] **12** Kisha miti ikauambia mzabibu, 'Wewe njoo, uwe malkia juu yetu.' **13** Ndipo mzabibu ukaiambia, 'Je, niiache divai yangu mpya ambayo humfurahisha Mungu na wanadamu,[c] na je, niende kuwayawaya juu ya miti?' **14** Mwishowe miti mingine yote ikauambia mkwamba,[d] 'Wewe njoo, uwe mfalme juu yetu.' **15** Ndipo mkwamba ukaiambia miti, 'Ikiwa kweli mnanitia mafuta niwe mfalme juu yenu, njooni, tafuteni kimbilio chini ya kivuli changu.[e] Lakini kama sivyo, moto[f] na utoke ndani ya mkwamba uiteketeze mierezi[g] ya Lebanoni.'[h]

16 "Na sasa ikiwa mmetenda kwa ukweli na bila kosa, mkamfanya Abimeleki kuwa mfalme,[i] na ikiwa wema ndio mmemwonyesha Yerubaali na nyumba yake, na ikiwa mmemtendea sawasawa na matendo ya mikono yake, **17** wakati baba yangu alipowapigania[j] ninyi, akaihatarisha nafsi[k] yake ili apate kuwakomboa ninyi kutoka katika mkono wa Midiani;[l] **18** nanyi, kwa upande wenu, mmesimama juu ya nyumba ya baba yangu leo ili mpate kuwaua wanawe,[m] watu 70,[n] juu ya jiwe moja, na ili mpate kumfanya Abimeleki, mwana wa kijakazi wake,[o] kuwa mfalme[p] juu ya wenye mashamba wa Shekemu kwa sababu tu yeye ni ndugu yenu; **19** ndiyo, ikiwa mmemtendea Yerubaali na nyumba yake kwa ukweli na bila kosa leo hii, shangilieni juu

SURA 9

a Mwa 29:14
1Nya 11:1
b 2Sa 15:6
c Amu 8:31
d Amu 8:33
Amu 9:46
e 2Nya 13:7
Mdo 17:5
f Amu 6:11
Amu 8:27
g 2Fa 11:1
2Nya 21:4
h Amu 9:20
i Kum 17:14
Amu 8:22
1Sa 8:7
j Mwa 35:4
Yos 24:26
k Amu 9:1
l Kum 11:29
Yos 8:33
Yoh 4:20
m Ho 14:6
n Amu 8:22
o Kut 29:2
Law 2:1
p Met 29:23
Mt 23:12
Ro 12:16

Safu ya 2

a Yoe 2:22
b Met 16:19
c Zb 104:15
Met 31:6
Mhu 2:3
Mhu 10:19
d Amu 9:6
2Fa 14:9
Zb 58:9
Met 15:25
Met 16:18
e Amu 9:19
Ga 6:3
f Amu 9:20
Amu 9:45
Amu 9:49
Isa 13:11
g 2Fa 14:9
Isa 2:13
Isa 37:24
Eze 31:3
Amo 2:9
Zek 11:2
h Kum 11:24
Yos 1:4
i Kum 17:15
Amu 9:6
Amu 9:15
j Amu 7:9
k Est 4:16
Ro 16:4
l Amu 8:28
Zb 83:9
m Amu 9:5
n Amu 8:30
o Amu 8:31
p Amu 9:6

ya Abimeleki naye pia ashangi-
lie juu yenu.[a] **20** Lakini kama
sivyo, moto[b] na utoke ndani ya
Abimeleki, uwateketeze wenye
mashamba wa Shekemu na nyu-
mba ya Milo,[c] kisha moto[d] na
utoke ndani ya wenye masha-
mba wa Shekemu na nyumba
ya Milo, nao umteketeze Abime-
leki."[e]

21 Ndipo Yothamu[f] akapiga
mbio, akakimbia, akaenda mpa-
ka Beeri, akaanza kukaa hapo
kwa sababu ya Abimeleki ndu-
gu yake.

22 Naye Abimeleki akae-
ndelea kujitwalia ukuu juu ya
Israeli kwa miaka mitatu.[g]
23 Ndipo Mungu akaacha roho
mbaya[h] itokee kati ya Abime-
leki na wale wenye mashamba
wa Shekemu, na hao wenye ma-
shamba wa Shekemu wakamte-
ndea Abimeleki hila,[i] **24** ili je-
uri iliyotendewa wale wana 70
wa Yerubaali ije[j] na kwamba
apate kuweka damu yao juu ya
Abimeleki ndugu yao kwa sa-
babu aliwaua,[k] na juu ya wenye
mashamba wa Shekemu kwa
sababu waliitia nguvu miko-
no[l] yake ili awaue ndugu zake.
25 Basi wenye mashamba wa
Shekemu wakaweka watu wa-
mvizie juu ya vilele vya milima,
nao wakawa wanamnyang'a-
nya vitu kila mtu ambaye alipi-
ta kando yao barabarani. Baa-
da ya muda Abimeleki akalete-
wa habari.

26 Ndipo Gaali[m] mwana wa
Ebedi na ndugu zake wakaja
na kuvuka kuingia Shekemu,[n]
nao wenye mashamba wa
Shekemu wakaanza kumtumai-
ni.[o] **27** Nao wakatoka kwenda
shambani kama kawaida, wa-
kakusanya zabibu za masha-
mba yao na kuzikanyaga na ku-
sherehekea kwa furaha,[p] ki-
sha wakaingia katika nyumba
ya mungu wao,[a] wakala na ku-
nywa[b] na kumlaani[c] Abimele-
ki. **28** Ndipo Gaali mwana wa
Ebedi akasema: "Abimeleki[d] ni
nani, na Shekemu ni nani ili tu-
mtumikie? Je, yeye si mwa-
na wa Yerubaali,[e] na je, Zebu-
li[f] si mjumbe wake? Ninyi we-
ngine watumikieni watu wa
Hamori,[g] baba ya Shekemu, la-
kini je, kwa nini sisi tumtumi-
kie? **29** Laiti watu hawa wa-
ngekuwa mkononi mwangu![h]
Ndipo ningemwondoa Abime-
leki." Naye akamwambia Abime-
leki: "Zidisha jeshi lako kwa wi-
ngi, kisha utoke nje."[i]

30 Naye Zebuli mkuu wa jiji
akayasikia maneno ya Gaali
mwana wa Ebedi.[j] Ndipo hasira
yake ikawaka. **31** Kwa hiyo
akatuma wajumbe waende kwa
Abimeleki kwa siri, akisema:
"Tazama! Gaali mwana wa Ebe-
di na ndugu zake sasa wame-
kuja Shekemu,[k] nao wanaliku-
sanya jiji kupigana na wewe.
32 Na sasa simama wakati wa
usiku,[l] wewe pamoja na watu
walio nawe, nanyi mvizie[m] sha-
mbani. **33** Na itatukia kwa-
mba wakati wa asubuhi mara
jua linapowaka mwamke mape-
ma, nanyi mfanye mashambuli-
zi ya ghafula juu ya jiji; na yeye
na wale watu walio pamoja naye
watakapotoka nje kupigana na
wewe, umtendee kadiri ya uwe-
zo wa mkono wako."

34 Basi Abimeleki na watu
wote waliokuwa pamoja naye
wakaondoka usiku, wakaanza
kulivizia jiji la Shekemu waki-
wa vikosi vinne. **35** Baadaye
Gaali[n] mwana wa Ebedi akato-
ka nje na kusimama penye mwi-
ngilio wa lango la jiji. Ndipo Abi-
meleki na watu waliokuwa pa-
moja naye wakasimama kutoka

SURA 9

a Met 10:28
Met 29:2
b Amu 9:15
c Amu 9:6
Amu 9:45
Amu 9:49
d Zb 28:4
e Amu 9:39
Amu 9:53
f Amu 9:5
g Met 28:2
h 1Sa 16:14
1Fa 12:15
i Met 13:15
Isa 33:1
Mt 7:2
Ga 6:7
j Kum 32:35
1Sa 15:33
Est 9:25
k Mwa 9:6
Hes 35:16
Amu 9:5
1Fa 2:32
Zb 7:16
Mt 23:35
l Kut 23:7
Amu 9:3
m Amu 9:28
Amu 9:41
n Mwa 33:18
Mwa 35:4
Yos 21:21
Yos 24:1
Amu 9:1
o Zb 146:3
p Isa 16:10
Yer 25:30
Yer 48:33

Safu ya 2

a Amu 8:33
Amu 9:4
Amu 9:46
b Kut 32:6
Da 5:4
Amo 2:8
c 1Sa 17:43
2Sa 16:5
Zb 4:4
Zb 39:1
d 1Sa 25:10
2Sa 20:1
1Fa 12:16
e Amu 6:32
1Sa 12:11
f Amu 9:41
g Mwa 34:2
h 2Sa 15:4
Zb 10:3
Ro 1:30
i Met 30:33
j Amu 9:26
k Yos 21:21
Yos 24:1
Amu 8:31
l Ayu 24:14
m Yos 8:4
n Amu 9:26

mahali pa kuvizia. **36** Gaali
alipoona watu hao, mara moja
akamwambia Zebuli: "Tazama!
Watu wanashuka kutoka kati-
ka vilele vya milima." Lakini
Zebuli akamwambia: "Ni vivu-
li vya milima unavyoviona kana
kwamba ni watu."[a]
37 Baadaye Gaali akasema
mara nyingine tena: "Tazama!
Watu wanashuka kutoka ka-
tikati ya nchi, na kikosi ki-
moja kinakuja kupitia njia ya
mti mkubwa wa Meonenimu."
38 Ndipo Zebuli akamwambia:
"Basi sasa yako wapi yale ma-
neno yako uliyosema,[b] 'Abime-
leki ni nani ili tumtumikie?'[c] Je,
hawa si wale watu ambao uli-
kataa?[d] Tafadhali, sasa toka nje
upigane nao."
39 Basi Gaali akatoka nje
mbele ya wenye mashamba wa
Shekemu, akapigana na Abi-
meleki. **40** Na Abimeleki aka-
mfuatilia, naye akakimbia mbe-
le yake; na waliouawa wakazidi
kuanguka kwa wingi mpaka pe-
nye mwingilio wa lango.
41 Na Abimeleki akaendelea
kukaa katika Aruma, naye Ze-
buli[e] akawafukuza Gaali[f] na
ndugu zake wasikae katika She-
kemu.[g] **42** Na ikawa kesho
yake kwamba watu wakaanza
kutoka nje kwenda shambani.
Basi wakamwambia Abimeleki.[h]
43 Kwa hiyo, akawachu-
kua watu na kuwagawanya
wawe vikosi vitatu,[i] akaanza
kuvizia shambani. Ndipo aka-
angalia, na tazama, watu wali-
kuwa wakitoka nje ya jiji. Basi
akaenda juu yao, akawapiga na
kuwaua. **44** Na Abimeleki na
vile vikosi vilivyokuwa pamoja
naye wakaenda mbio ili wapate
kusimama penye mwingilio wa
lango la jiji, huku vikosi viwi-
li vikienda mbio kuwapiga wote

SURA 9
a Amu 9:32
b Zb 94:4
Met 21:24
Yak 3:5
c Amu 9:28
d Amu 9:29
e Amu 9:30
f Amu 9:26
g Mwa 35:4
Yos 21:21
Yos 24:1
h Amu 8:31
Amu 9:1
Amu 9:6
i Met 20:18

Safu ya 2
a Amu 9:15
b Amu 9:20
c 1Fa 12:25
d Kum 29:23
Ayu 39:6
Zb 107:34
Yer 17:6
e Amu 8:33
Amu 9:4
Amu 9:27
f Zb 68:14
g Amu 7:17
h Amu 9:15
Amu 9:20
i 2Sa 11:21
j Amu 9:48
Amu 9:49

waliokuwa shambani, nao wa-
kawapiga na kuwaua.[a] **45** Na
Abimeleki akapigana na jiji hilo
siku hiyo nzima, akaliteka jiji;
akawaua watu waliokuwa ndani
yake,[b] kisha akalibomoa jiji[c] na
kulitia chumvi.[d]
46 Wakati wenye mashamba
wote wa Shekemu waliposi-
kia habari hizo, wakaenda ha-
raka katika ngome ya nyumba
ya El-berithi.[e] **47** Ndipo Abi-
meleki akaletewa habari kwa-
mba wenye mashamba wote
wa Shekemu wamekusanyika
pamoja. **48** Kwa hiyo Abime-
leki akapanda Mlima Salmo-
ni,[f] yeye na watu wote walio-
kuwa pamoja naye. Basi Abime-
leki akachukua shoka mkono-
ni mwake, akakata tawi la mti,
akaliinua na kuliweka begani
pake, akawaambia watu walio-
kuwa pamoja naye: "Mlivyoona
nikifanya—fanyeni hivyo, ha-
raka, kama mimi!"[g] **49** Basi
watu wote wakajikatia tawi kila
mmoja wao, wakamfuata Abi-
meleki. Ndipo wakayaweka juu
ya ngome ile, nao wakaitia moto
ngome hiyo juu yao, hivi kwa-
mba watu wote wa mnara wa
Shekemu wakafa pia, karibu
watu elfu moja, wanaume na
wanawake.[h]
50 Na Abimeleki akaenda
Thebesi,[i] akapiga kambi juu
ya Thebesi, akaliteka. **51** Na
kwa vile kulikuwa na mnara
wenye nguvu katikati ya jiji,
wanaume wote na wanawake
na wenye mashamba wote wa
jiji walikimbilia humo, kisha
wakaufunga nyuma yao na ku-
panda juu ya paa ya mnara huo.
52 Naye Abimeleki akaondo-
ka akaenda kwenye mnara huo
na kuanza kupigana nao, akae-
nda karibu na mlango wa mna-
ra ili kuuteketeza kwa moto.[j]

53 Ndipo mwanamke fulani
akatupa jiwe la juu la kusagia
juu ya kichwa cha Abimeleki,
akalivunja fuvu la kichwa cha-
ke vipande-vipande.[a] **54** Kwa
hiyo, akamwita haraka mtumi-
shi aliyechukua silaha zake na
kumwambia: "Chomoa upanga
wako, uniue,[b] wasije wakase-
ma juu yangu, 'Mwanamke ndi-
ye aliyemuua.'" Mara moja mtu-
mishi wake akamchoma, naye
akafa.[c]
55 Watu wa Israeli walipoo-
na kwamba Abimeleki ameku-
fa, basi wakaenda kila mmo-
ja wao mahali pake. **56** Hi-
vyo Mungu akaurudisha uovu
wa Abimeleki aliomtendea baba
yake kwa sababu ya kuwaua
ndugu zake 70.[d] **57** Na Mu-
ngu akaurudisha uovu wote wa
watu wa Shekemu juu ya vi-
chwa vyao wenyewe, ili ile laa-
na[e] ya Yothamu[f] mwana wa Ye-
rubaali[g] ije juu yao.[h]

10 Na baada ya Abimeleki,
akasimama Tola mwana
wa Pua, mwana wa Dodo, mtu
wa Isakari, ili kuwaokoa[i] Isra-
eli, naye alikuwa akikaa Sha-
miri katika eneo lenye milima
la Efraimu.[j] **2** Naye akaende-
lea kuhukumu Israeli kwa mia-
ka 23, kisha akafa, akazikwa ka-
tika Shamiri.
3 Ndipo baada yake Yairi
Mgileadi[k] akasimama, naye aka-
endelea kuhukumu Israeli
kwa miaka 22. **4** Naye akaja
kuwa na wana 30 waliopanda
punda 30 waliokomaa,[l] nao wa-
likuwa na majiji 30. Majiji hayo
wanaendelea kuyaita Hawoth-
yairi[m] mpaka leo hii; yako ka-
tika nchi ya Gileadi. **5** Kisha
Yairi akafa, akazikwa katika
Kamoni.
6 Na wana wa Israeli waka-
anza tena kufanya yaliyokuwa
mabaya machoni pa Yehova,[a]
nao wakaanza kutumikia Ma-
baali[b] na sanamu za Ashtore-
thi[c] na miungu ya Siria[d] na mi-
ungu ya Sidoni[e] na miungu ya
Moabu[f] na miungu ya wana wa
Amoni[g] na miungu ya Wafili-
sti.[h] Basi wakamwacha Yeho-
va wala hawakumtumikia yeye.[i]
7 Hivyo hasira ya Yehova ika-
waka juu ya Israeli,[j] naye aka-
wauza[k] mkononi mwa Wafili-
sti[l] na mkononi mwa wana wa
Amoni.[m] **8** Kwa hiyo wakawa-
vunja-vunja na kuwakandami-
za sana wana wa Israeli mwaka
huo—kwa miaka kumi na mi-
nane wana wote wa Israeli wali-
okuwa ng'ambo ya Yordani kati-
ka nchi ya Waamori iliyokuwa
katika Gileadi. **9** Na wana wa
Amoni wakawa wakivuka Yor-
dani ili kupigana na Yuda na
Benyamini na nyumba ya Efra-
imu; na Israeli walikuwa kati-
ka taabu kubwa sana.[n] **10** Na
wana wa Israeli wakaanza ku-
mwomba Yehova msaada,[o] wa-
kisema: "Tumekutendea dha-
mbi,[p] kwa sababu tumemwa-
cha Mungu wetu nasi tunatumi-
kia Mabaali."[q]
11 Ndipo Yehova akawaam-
bia wana wa Israeli: "Je, mimi
sikuwaokoa ninyi kutoka Misri[r]
na kutoka mkononi mwa Wa-
amori[s] na wana wa Amoni[t] na
Wafilisti[u] **12** na Wasidoni[v] na
Amaleki[w] na Midiani,[x] walipo-
wakandamiza,[y] nanyi mkanili-
lia, nami nikawaokoa kutoka
katika mkono wao? **13** Lakini
ninyi, mliniacha,[z] mkaanza kui-
tumikia miungu mingine.[a] Ndi-
yo sababu sitawaokoa tena.[b]
14 Nendeni mwombe msaada
kutoka kwa miungu[c] ambayo

SURA 9
a Amu 4:9; Amu 5:26; 2Sa 11:21; 2Sa 20:22; Ayu 31:3
b 1Sa 31:4
c Zb 37:2
d Mwa 9:6; Amu 9:5; Amu 9:24; 1Sa 25:39; Zb 58:10; Zb 94:23; Met 5:22; Ga 6:7
e Amu 9:20
f Amu 9:7
g Amu 6:32; Amu 7:1; Amu 8:35
h Amu 9:45

SURA 10
i Amu 2:16
j Yos 17:15
k Mwa 31:48; Hes 32:29
l Amu 5:10; Amu 12:14
m Kum 3:14

Safu ya 2
a Kum 28:15; Amu 2:11; Amu 2:19; Amu 4:1; Amu 6:1; Ne 9:28
b Amu 3:7; Zb 106:36; Zb 106:38
c Kum 27:15; Amu 2:13; 1Sa 7:3
d Amu 2:12; 2Nya 28:23
e 1Fa 11:33; 1Fa 16:31
f Hes 25:2; Ru 1:15; 2Fa 23:13
g 1Fa 11:5
h Amu 16:23; 1Sa 5:4; 2Fa 1:2
i Kum 32:18; 2Nya 15:2
j Law 26:18; Kum 31:17; Amu 2:14
k Kum 28:48; Amu 4:2; Zb 44:12
l 1Sa 12:9
m Hes 33:56; Amu 3:13
n Kum 28:25; 2Nya 15:6
o Kum 4:30; Amu 2:18; Zb 106:44; Zb 107:13
p 1Sa 12:10
q Amu 2:13; Amu 3:7
r Kut 14:30; 1Sa 12:8; Zb 78:51; Ebr 11:29
s Hes 21:25; Zb 135:11
t Amu 3:13
u Amu 3:31
v Amu 3:3; Amu 5:19;
w Amu 6:3;
x Amu 6:1;
y Zb 106:42;
z Kum 32:15; 2Nya 15:2;
a Amu 2:12;
b Omb 3:44; Mik 3:4;
c Zb 115:6; Isa 45:20; Isa 46:7.

mmechagua.[a] Hiyo na iwaokoe wakati wa taabu yenu.”
15 Lakini wana wa Israeli wakamwambia Yehova: “Tumetenda dhambi.[b] Wewe mwenyewe ututendee kulingana na lolote lililo jema machoni pako.[c] Lakini tafadhali, utukomboe tu leo hii.”[d] **16** Nao wakaanza kuiondoa miungu ya kigeni kutoka katikati yao,[e] na kumtumikia Yehova,[f] hivi kwamba nafsi[g] yake ikawa haina subira kwa sababu ya taabu ya Israeli.[h]

17 Baadaye wana wa Amoni[i] wakakusanywa pamoja, wakapiga kambi katika Gileadi.[j] Kwa hiyo wana wa Israeli wakajikusanya pamoja, wakapiga kambi katika Mispa.[k] **18** Ndipo watu na wakuu wa Gileadi wakaanza kuambiana: “Ni nani atakayeongoza katika kupigana na wana wa Amoni?[l] Huyo na awe kichwa juu ya wakaaji wote wa Gileadi.”[m]

11 Basi Yeftha[n] Mgileadi[o] akawa mwanamume mwenye nguvu na shujaa,[p] naye alikuwa ni mwana wa mwanamke kahaba,[q] naye Gileadi akamzaa Yeftha. **2** Na mke wa Gileadi akaendelea kumzalia wana. Wakati wana wa mke yule walipokuwa wakubwa, wakamfukuza Yeftha na kumwambia: “Usiwe na urithi wowote katika nyumba ya baba yetu,[r] kwa sababu wewe ni mwana wa mwanamke mwingine.” **3** Basi Yeftha akakimbia kwa sababu ya ndugu zake, akaenda kukaa katika nchi ya Tobu.[s] Kisha watu wanaozurura-zurura wakaendelea kujikusanya pamoja kwa Yeftha, nao wakawa wakienda nje pamoja naye.[t]

4 Na ikawa baada ya muda kwamba wana wa Amoni wakaanza kupigana na Israeli.[a] **5** Ikawa kwamba wana wa Amoni walipopigana na Israeli,[b] wanaume wazee wa Gileadi wakaenda mara moja kumchukua Yeftha kutoka katika nchi ya Tobu.[c] **6** Nao wakamwambia Yeftha: “Njoo uwe kiongozi wetu, nasi tupigane na wana wa Amoni.” **7** Lakini Yeftha akawaambia wanaume wazee[d] wa Gileadi: “Je, si ninyi mlionichukia, mkanifukuza kutoka nyumbani kwa baba yangu?[e] Kwa nini basi mmenijia hivi sasa mkiwa katika taabu?”[f] **8** Ndipo wanaume wazee wa Gileadi wakamwambia Yeftha: “Ndiyo sababu sasa tumerudi kwako,[g] nawe uende pamoja nasi na kupigana na wana wa Amoni, nawe uwe kwetu kichwa juu ya wakaaji wote wa Gileadi.”[h] **9** Basi Yeftha akawaambia wanaume wazee wa Gileadi: “Ikiwa mnanirudisha ili kupigana na wana wa Amoni, na Yehova akiwatia[i] mkononi mwangu, mimi mwenyewe nitakuwa kichwa chenu!” **10** Ndipo wanaume wazee wa Gileadi wakamwambia Yeftha: “Yehova na awe msikilizaji kati yetu[j] ikiwa hatutafanya kulingana na neno lako.”[k] **11** Basi Yeftha akaenda pamoja na wanaume wazee wa Gileadi, na watu wakamweka juu yao awe kichwa na kiongozi.[l] Na Yeftha akasema maneno yake yote mbele za Yehova[m] katika Mispa.[n]

12 Ndipo Yeftha akatuma wajumbe kwa mfalme wa wana wa Amoni,[o] akisema: “Nina nini na wewe,[p] kwa kuwa umekuja juu yangu ili kupigana katika nchi yangu?” **13** Basi mfalme wa wana wa Amoni akawaambia wale wajumbe wa Yeftha: “Ni kwa sababu Israeli

SURA 10

a Kum 32:37; 1Fa 18:27; Yer 2:28
b 1Fa 8:46; Yer 3:25
c 1Sa 3:18; 1Sa 12:10; 2Sa 15:26
d Kum 4:29; Amu 10:8
e Kum 7:26; 2Nya 7:14; 2Nya 15:8; 2Nya 33:15
f Kut 20:2; Yer 18:8
g Law 26:11; Isa 1:14; Isa 42:1
h 2Nya 33:13; Zb 106:44; Isa 63:9; Yer 31:20
i Mwa 19:38; Amu 3:13; Amu 10:7
j Mwa 31:21; Hes 32:29
k Amu 11:29
l Amu 11:1
m Amu 11:11; Amu 12:7

SURA 11

n 1Sa 12:11; Ebr 11:32
o Amu 12:7
p Amu 6:12; 2Fa 5:1
q Yos 2:1; 1Ko 6:11
r Mwa 21:10; Kum 21:15
s Amu 11:5
t 1Sa 22:2

Safu ya 2

a Amu 10:17
b Amu 10:9
c Amu 11:3
d Yos 20:4; Amu 8:14
e Mwa 26:27; Kum 21:17; Amu 11:2
f Met 17:17
g Lu 17:4
h Amu 10:18
i Kum 7:23; Zb 44:3; Met 3:6
j Mwa 31:50; 1Sa 12:5; Yer 42:5
k Kut 20:7; Law 19:12
l Amu 11:8
m Kum 6:13
n Amu 10:17; Amu 11:34
o Mwa 19:38; Amu 10:17
p Yos 22:24; 2Sa 16:10

walichukua nchi yangu walipopanda kutoka Misri,[a] kuanzia Arnoni[b] mpaka Yaboki na mpaka Yordani.[c] Basi sasa irudishe kwa amani." **14** Lakini Yeftha akatuma wajumbe tena kwa mfalme wa wana wa Amoni **15** na kumwambia:

"Yeftha amesema hivi, 'Israeli hawakuchukua nchi ya Moabu[d] wala nchi ya wana wa Amoni.[e] **16** Kwa maana Israeli walipopanda kutoka Misri, walitembea kupitia nyika mpaka Bahari Nyekundu,[f] wakaja Kadeshi.[g] **17** Ndipo Israeli wakatuma wajumbe kwa mfalme wa Edomu,[h] wakisema: "Tafadhali, niache nipite katika nchi yako," naye mfalme wa Edomu hakusikiliza. Pia wakatuma wajumbe kwa mfalme wa Moabu,[i] naye hakukubali. Basi Israeli wakaendelea kukaa katika Kadeshi.[j] **18** Walipotembea kupitia nyika, waliizunguka nchi ya Edomu[k] na nchi ya Moabu, nao wakaenda upande wa mashariki wa nchi ya Moabu,[l] wakakaa katika eneo la Arnoni; nao hawakuja katika mpaka wa Moabu,[m] kwa sababu Arnoni ulikuwa ni mpaka wa Moabu.[n]

19 "'Baada ya hayo Israeli wakatuma wajumbe kwa Sihoni mfalme wa Waamori, mfalme wa Heshboni,[o] na Israeli wakamwambia: "Tafadhali, tuache tupite katika nchi yako kwenda mahali pangu mwenyewe."[p] **20** Naye Sihoni hakuwaamini Israeli kwamba wavukie katika eneo lake, na Sihoni akakusanya watu wake wote pamoja, akapiga kambi katika Yahazi,[q] wakapigana na Israeli.[r] **21** Kwa hiyo Yehova Mungu wa Israeli akamtia Sihoni na watu wake wote mkononi mwa Israeli, nao wakawapiga na Israeli wakaimiliki nchi yote ya Waamori waliokuwa wakikaa katika nchi hiyo.[a] **22** Kwa hiyo wakarithi eneo lote la Waamori kutoka Arnoni mpaka Yaboki na kutoka ile nyika mpaka Yordani.[b]

23 "'Na sasa Yehova Mungu wa Israeli ndiye aliyewafukuza Waamori kutoka mbele ya watu wake Israeli,[c] nawe kwa upande wako, unataka kuwafukuza. **24** Je, hutamfukuza yule ambaye Kemoshi[d] mungu wako anakufanya umfukuze? Na kila mmoja ambaye Yehova Mungu wetu amemfukuza mbele yetu ndiye tutakayemfukuza.[e] **25** Na sasa je, wewe ni bora kuliko Balaki mwana wa Sipori, mfalme wa Moabu?[f] Je, alipata kushindana na Israeli, au je, alipata kupigana nao? **26** Wakati Israeli walipokuwa wakikaa katika Heshboni na miji yake ya kandokando[g] na katika Aroeri[h] na miji yake ya kandokando na katika majiji yote yaliyo kando ya kingo za Arnoni kwa miaka mia tatu, kwa nini, basi, hamkuinyakua wakati huo?[i] **27** Kwa upande wangu, mimi sikukutendea dhambi, lakini wewe unanitendea vibaya kwa kupigana nami. Yehova aliye Mwamuzi[j] na ahukumu leo kati ya wana wa Israeli na wana wa Amoni.'"

28 Na mfalme wa wana wa Amoni hakuyasikiliza maneno ya Yeftha ambayo alikuwa amemtumia.[k]

29 Sasa roho ya Yehova ikaja juu ya Yeftha,[l] naye akapita katika Gileadi na Manase, akapita katika Mispe la Gileadi,[m] na kutoka Mispe la Gileadi akapita kwenda kwa wana wa Amoni.

30 Ndipo Yeftha akaweka nadhiri[n] kwa Yehova na kuse-

SURA 11

a Hes 21:24
Met 19:5
b Hes 21:26
c Kum 3:16
Kum 3:17
d Mwa 19:37
Kum 2:9
e Kum 2:19
Kum 2:37
2Nya 20:10
f Hes 14:25
Kum 1:40
g Mwa 16:14
Hes 20:1
h Mwa 36:1
Hes 20:14
Kum 2:4
i Mwa 19:37
Kum 2:9
j Hes 20:22
k Hes 21:4
l Hes 21:11
m Hes 21:13
n Hes 22:36
o Hes 21:21
Kum 2:26
Yos 13:10
p Hes 21:22
Kum 2:27
q Kum 2:32
r Hes 21:23

Safu ya 2

a Hes 21:24
Kum 2:33
Yos 13:15
Yos 13:21
Zb 135:11
b Kum 2:36
Yos 12:2
c Hes 21:26
Ne 9:22
d Hes 21:29
1Fa 11:7
Yer 48:7
e Kut 23:28
Kut 34:11
Hes 33:53
Kum 7:16
Kum 9:5
Kum 18:12
2Nya 20:7
Zb 44:2
f Hes 22:2
Kum 23:3
Yos 24:9
g Hes 21:25
Kum 2:24
Kum 3:2
Yos 12:2
Yos 13:10
h Kum 2:36
Kum 3:12
i Hes 21:26
j Mwa 18:25
1Sa 24:15
Isa 33:22
k Amu 11:14
l Amu 3:10
Zek 4:6
m Amu 10:17
n Mwa 28:20
Hes 30:2
Kum 23:21
1Sa 1:11
Mhu 5:4

ma: “Hakika ukiwatia wana
wa Amoni mkononi mwangu,
31 itatukia pia kwamba yule
atakayetoka nje, atakayetoka
nje ya milango ya nyumba ya-
ngu kuja kunipokea nitakapo-
rudi kwa amani[a] kutoka kwa
wana wa Amoni, lazima atak-
uwa wa Yehova,[b] nami nitamtoa
huyo kuwa toleo la kuteke-
tezwa.”[c]
32 Basi Yeftha akapita kwe-
nda kwa wana wa Amoni ili ku-
pigana nao, na Yehova akawa-
tia mkononi mwake. **33** Aka-
wapiga kwa mauaji makubwa
sana kutoka Aroeri mpaka Mi-
nithi,[d] majiji 20, na mpaka Abel-
keramimu. Basi wana wa Amo-
ni wakatiishwa mbele ya wana
wa Israeli.
34 Mwishowe Yeftha aka-
ja Mispa[e] nyumbani kwake,
na, tazama! binti yake akato-
ka nje kumpokea, akipiga tari
na kucheza dansi![f] Naye aliku-
wa ndiye mtoto pekee. Haku-
wa na mwana wala binti isi-
pokuwa yeye. **35** Na ikawa
kwamba alipomwona, akaanza
kuyararua mavazi[g] yake na ku-
sema: “Ole, binti yangu! Kwa
kweli umenifanya niiname chi-
ni, nawe mwenyewe umekuwa
ndiye yule ambaye nilikuwa ni-
kitenga. Mimi nimemfungulia
Yehova kinywa changu, nami
siwezi kurudi nyuma.”[h]
36 Lakini akamwambia:
“Baba yangu, ikiwa umemfu-
ngulia Yehova kinywa chako,
nitendee kulingana na neno li-
lilotoka katika kinywa chako,[i]
kwa kuwa Yehova amekulipizia
kisasi juu ya adui zako, wana wa
Amoni.” **37** Naye akaendelea
kumwambia baba yake: “Na ni-
fanyiwe jambo hili: Niache kwa
miezi miwili, niende, nami nita-
shuka milimani, na acha niuli-
lie ubikira wangu,[a] mimi pamo-
ja na wasichana wenzangu.”
38 Ndipo akasema: “Nenda!”
Basi akamwacha aende kwa mi-
ezi miwili; naye akaenda, yeye
pamoja na wasichana wenzake,
akiulilia ubikira wake juu ya
milima. **39** Na ikawa kwamba
mwishoni mwa miezi miwili,
akarudi kwa baba yake, kisha
baba yake akatimiza ile nadhi-
ri yake ambayo alikuwa ame-
weka kumwelekea.[b] Naye ha-
kupata kamwe kulala na mwa-
namume. Nayo ikawa sharti
katika Israeli: **40** Mwaka baa-
da ya mwaka binti za Israeli wa-
kawa wakienda kumpongeza bi-
nti ya Yeftha Mgileadi, siku nne
kwa mwaka.[c]

12 Ndipo watu wa Efraimu
wakakusanywa pamoja
na kuvuka kuelekea kaskazi-
ni, nao wakamwambia Yeftha:
“Kwa nini ulivuka kupigana
na wana wa Amoni, nawe hu-
kutuita twende pamoja nawe?[d]
Nyumba yako tutaiteketeza juu
yako kwa moto.”[e] **2** Lakini
Yeftha akawaambia: “Mimi na
watu wangu tulikuwa na ugo-
mvi mkubwa pamoja na wana
wa Amoni.[f] Nami nikawaomba
ninyi msaada, wala hamkuni-
okoa kutoka mkononi mwao.
3 Nilipoona kwamba hamnio-
koi, nikaazimia kuitia nafsi ya-
ngu mkononi[g] mwangu mwe-
nyewe, nikavuka kupigana na
wana wa Amoni.[h] Hivyo Yeho-
va akawatia mkononi mwangu.
Basi kwa nini mmekuja juu ya-
ngu kupigana nami leo?”
4 Basi bila kukawia Yeftha
akakusanya watu wote wa Gile-
adi,[i] akapigana na Efraimu; na
watu wa Gileadi wakapiga Efra-
imu, kwa maana walikuwa wa-
mesema: “Ninyi Gileadi ni watu
walioponyoka kutoka Efraimu,

SURA 11
a Mwa 28:21
Yos 10:21
b Amu 13:5
1Sa 1:11
1Sa 1:22
c Kum 18:10
1Sa 1:24
1Sa 1:28
Zb 66:13
Yer 7:31
d Eze 27:17
e Amu 10:17
Amu 11:11
f Kut 15:20
1Sa 18:6
Zb 68:25
g Mwa 37:34
h Zb 15:4
Zb 76:11
Mt 5:33
i Amu 11:30
Amu 11:31
Efe 6:1
Kol 3:20

Safu ya 2
a Mwa 24:16
Mwa 30:23
Ru 4:14
1Sa 1:6
b 1Sa 1:22
1Sa 1:24
c 1Ko 7:34
1Ko 7:37

SURA 12
d Amu 8:1
Met 8:13
Met 16:18
Yak 3:16
e Amu 14:15
Amu 15:6
2Nya 25:10
f Amu 11:6
Amu 11:9
g Amu 9:17
1Sa 19:5
1Sa 28:21
2Sa 23:17
Ayu 13:14
Zb 119:109
h Amu 11:29
i Kum 3:12
Kum 3:13

kutoka ndani ya Efraimu, kutoka ndani ya Manase." **5** Nao Gileadi wakateka vivuko vya Yordani[a] mbele ya Efraimu; ndipo ikatukia kwamba wakati watu wa Efraimu waliokuwa wakikimbia waliposema: "Niache nivuke," ndipo watu wa Gileadi wakawa wakimwambia kila mmoja wao: "Je, wewe ni Mwefraimu?" Akisema: "Hapana!" **6** ndipo walipomwambia: "Tafadhali sema Shibolethi."[b] Naye alisema: "Sibolethi," kwa kuwa hakuweza kutamka neno hilo kwa usahihi. Nao walimshika na kumuua kwenye vivuko vya Yordani. Basi wakati huo wakaanguka watu 42,000 kutoka katika Efraimu.[c]

7 Na Yeftha akaendelea kuhukumu Israeli kwa miaka sita, kisha Yeftha Mgileadi akafa, akazikwa katika jiji lake kule Gileadi.

8 Naye Ibzani kutoka Bethlehemu[d] akaanza kuhukumu Israeli baada yake.[e] **9** Naye akawa na wana 30 na binti 30. Akatuma watu nje kuleta binti 30 kwa ajili ya wanawe kutoka nje. Naye akaendelea kuhukumu Israeli kwa miaka saba. **10** Kisha Ibzani akafa, akazikwa Bethlehemu.

11 Na baada yake Eloni Mzabuloni[f] akaanza kuhukumu Israeli. Naye akaendelea kuhukumu Israeli kwa miaka kumi. **12** Kisha Eloni Mzabuloni akafa, akazikwa Aiyaloni katika nchi ya Zabuloni.

13 Na baada yake Abdoni mwana wa Hileli Mpirathoni[g] akaanza kuhukumu Israeli. **14** Naye akaja kuwa na wana 40 na wajukuu 30 waliopanda punda wakomavu[h] 70. Naye akaendelea kuhukumu Israeli kwa miaka minane. **15** Kisha Abdoni mwana wa Hileli Mpirathoni akafa, akazikwa Pirathoni katika nchi ya Efraimu katika mlima wa Mwamaleki.[a]

13 Wana wa Israeli wakaanza tena kufanya yaliyokuwa mabaya machoni pa Yehova,[b] na hivyo Yehova akawatia mkononi mwa Wafilisti[c] kwa miaka 40.

2 Wakati huo palikuwa na mtu mmoja wa Sora[d] wa familia ya Wadani,[e] na jina lake lilikuwa Manoa.[f] Na mke wake alikuwa tasa naye hakuwa amezaa mtoto yeyote.[g] **3** Ndipo malaika wa Yehova akamtokea huyo mwanamke,[h] akamwambia: "Tazama, sasa, wewe ni tasa nawe hujazaa mtoto yeyote. Nawe hakika utachukua mimba na kuzaa mwana.[i] **4** Basi sasa jiangalie, tafadhali, usinywe divai wala kileo,[j] wala usile kitu chochote kisicho safi.[k] **5** Kwa maana, tazama! utachukua mimba, nawe utazaa mwana, na wembe wowote usipite juu ya kichwa chake,[l] kwa maana mtoto huyo atakuwa Mnadhiri[m] wa Mungu tangu atakapotoka tumboni;[n] naye ndiye atakayeongoza katika kuokoa Israeli kutoka mkononi mwa Wafilisti."[o]

6 Ndipo mwanamke huyo akaenda, akamwambia mume wake: "Kuna mtu fulani wa Mungu wa kweli ambaye alinijia, na sura yake ilikuwa kama sura ya malaika wa Mungu wa kweli,[p] yenye kuogopesha sana.[q] Nami sikumuuliza mahali alikotoka, wala hakuniambia jina lake.[r] **7** Lakini aliniambia, 'Tazama! Utachukua mimba, nawe hakika utazaa mwana.[s] Basi sasa usinywe divai wala kileo, wala usile kitu chochote kisicho safi, kwa maana mtoto huyo atakuwa Mna-

SURA 12

a Yos 2:7
Amu 3:28
Amu 7:24
b Mt 26:73
c Met 16:5
Met 17:19
Mhu 10:12
d Yos 19:10
Yos 19:15
e Amu 2:16
f Mwa 30:20
Yos 19:10
Amu 5:14
g Amu 12:15
2Sa 23:30
1Nya 27:14
h Amu 5:10
Amu 10:4

Safu ya 2

a Mwa 36:12
Kut 17:16
Hes 13:29
1Sa 15:2

SURA 13

b Amu 2:11
Amu 2:19
Amu 10:6
c Kut 13:17
Yos 13:2
Yos 13:3
Amu 10:7
1Sa 12:9
d Yos 15:33
Yos 19:41
2Nya 11:10
e Mwa 49:16
Kum 33:22
Yos 19:40
f Amu 16:31
g Mwa 16:1
Mwa 25:21
Lu 1:7
h Mwa 16:7
Lu 1:11
i Mwa 18:10
1Sa 1:20
2Fa 4:16
Lu 1:13
j Hes 6:3
Lu 1:15
k Law 11:27
Law 11:47
l Hes 6:5
1Sa 1:11
m Hes 6:2
Amu 16:17
n Lu 1:15
o Amu 2:16
Amu 13:1
Ne 9:27
p Mt 28:3
Mdo 6:15
q Mwa 28:17
Kut 3:6
Da 8:17
r Mwa 32:29
Amu 13:17
Amu 13:18
s Amu 13:3

dhiri wa Mungu tangu atakapotoka tumboni mpaka siku ya kufa kwake.'"[a]

8 Na Manoa akaanza kumsihi Yehova, akisema: "Nakuomba radhi, Yehova.[b] Tafadhali, yule mtu wa Mungu wa kweli ambaye ulimtuma na arudi kwetu tena, atufundishe[c] yale tunayopaswa kumtendea huyo mtoto atakayezaliwa."[d] **9** Basi Mungu wa kweli akaisikiliza sauti ya Manoa,[e] na yule malaika wa Mungu wa kweli akamjia tena yule mwanamke alipokuwa ameketi shambani, lakini Manoa mume wake hakuwa pamoja naye. **10** Bila kukawia huyo mwanamke akafanya haraka na kukimbia, akamwambia mume[f] wake na kusema: "Tazama! Yule mtu aliyenijia siku ile amenitokea."[g]

11 Kwa hiyo Manoa akasimama, akafuatana na mke wake, akamjia yule mtu na kumwambia: "Je, wewe ndiye yule mtu aliyesema na huyu mwanamke?"[h] naye akajibu: "Ni mimi." **12** Ndipo Manoa akasema: "Basi maneno yako na yatimie. Mtoto huyo ataishi maisha ya aina gani, naye atafanya kazi gani?"[i] **13** Basi malaika wa Yehova akamwambia Manoa: "Kila jambo ambalo nilimtajia huyu mwanamke ajiepushe nalo.[j] **14** Asile kitu chochote kinachotokana na mzabibu wa divai, wala asinywe divai yoyote wala kileo,[k] wala asile kitu chochote kisicho safi.[l] Naye ashike kila jambo ambalo nimemwamuru."[m]

15 Sasa Manoa akamwambia malaika wa Yehova: "Tafadhali, acha tukuzuilie, tukuandalie mwana-mbuzi."[n] **16** Lakini malaika wa Yehova akamwambia Manoa: "Ukinizuilia, sitakula mkate wako; bali ukitaka kutoa toleo la kuteketezwa kwa Yehova,[a] unaweza kulitoa." Kwa maana Manoa hakujua kwamba huyo alikuwa ni malaika wa Yehova. **17** Kisha Manoa akamwambia malaika wa Yehova: "Jina lako ni nani,[b] ili neno lako litakapotimia, tukupe heshima?" **18** Hata hivyo, malaika wa Yehova akamwambia: "Kwa nini unauliza juu ya jina langu, wakati jina hilo ni la ajabu?"

19 Basi Manoa akachukua mwana-mbuzi na toleo la nafaka, akamtolea Yehova juu ya mwamba.[c] Naye huyo alikuwa akifanya jambo fulani kwa njia ya ajabu huku Manoa na mke wake wakitazama. **20** Basi ikawa kwamba, mwali wa moto ulipokuwa ukipaa kutoka katika madhabahu kuelekea mbinguni, malaika wa Yehova akapaa katika ule mwali wa madhabahu huku Manoa na mke wake wakitazama.[d] Wakaanguka kifudifudi mara moja.[e] **21** Na malaika wa Yehova hakumtokea tena Manoa na mke wake. Ndipo Manoa akajua kwamba huyo alikuwa ni malaika wa Yehova.[f] **22** Basi Manoa akamwambia mke wake: "Hakika tutakufa,[g] kwa sababu yule ambaye tumemwona ni Mungu."[h] **23** Lakini mke wake akamwambia: "Ikiwa Yehova alitaka tu kutuua, basi hangekubali toleo la kuteketezwa na toleo la nafaka kutoka mkononi mwetu,[i] naye hangetuonyesha mambo haya yote, naye kufikia sasa hangetuacha tusikie jambo lolote kama hili."[j]

24 Baadaye huyo mwanamke akazaa mwana, akamwita jina Samsoni;[k] na mvulana huyo akazidi kukua, na

SURA 13

a Amu 13:4
b Kut 4:10
Amu 6:15
c Met 3:6
Met 16:20
d Kum 4:9
Kum 6:7
e Zb 65:2
Zb 66:19
f 1Ko 11:3
Efe 5:24
1Pe 3:5
g Amu 13:3
h Amu 13:5
i Mwa 18:19
Amu 13:8
Met 22:6
Efe 6:4
j Amu 13:4
k Hes 6:3
l Law 11:27
Law 11:47
m Kum 12:32
n Mwa 18:5
Mwa 18:7
Amu 6:18
Ebr 13:2

Safu ya 2

a Amu 6:26
b Mwa 32:29
Amu 13:6
c Amu 6:20
d Mdo 1:9
e Mwa 17:3
1Nya 21:16
Mt 17:6
f Amu 6:22
g Amu 6:23
h Mwa 16:7
Mwa 16:13
Mwa 32:24
Mwa 32:30
Kut 33:20
Yoh 1:18
i Mwa 4:4
Amu 13:16
j Zb 25:14
Met 3:32
k Ebr 11:32

Yehova akaendelea kumbariki.[a]
25 Baada ya muda roho ya Yehova[b] ikaanza kumchochea katika Mahane-dani[c] kati ya Sora[d] na Eshtaoli.[e]

14 Ndipo Samsoni akashuka mpaka Timna,[f] akamwona mwanamke mmoja huko Timna kati ya binti za Wafilisti. **2** Basi akapanda, akamwambia baba yake na mama yake, akisema: "Nimemwona mwanamke mmoja huko Timna kati ya binti za Wafilisti, basi sasa mniletee mwanamke huyo awe mke wangu."[g] **3** Lakini baba yake na mama yake wakamwambia: "Je, hakuna mwanamke yeyote kati ya binti za ndugu zako na kati ya watu wangu wote,[h] hivi kwamba uende kumchukua mwanamke kutoka kwa Wafilisti wasiotahiriwa?"[i] Lakini bado Samsoni akamwambia baba yake: "Nileteeni huyo, kwa maana ndiye anayestahili kabisa machoni pangu." **4** Lakini baba yake na mama yake hawakujua kwamba jambo hilo lilitoka kwa Yehova,[j] kwamba alikuwa akitafuta nafasi ya kuwapiga Wafilisti, kwa kuwa wakati huo hasa Wafilisti walikuwa wakitawala juu ya Israeli.[k]

5 Basi Samsoni akashuka pamoja na baba yake na mama yake, wakaenda Timna.[l] Alipofika katika mashamba ya mizabibu ya Timna, tazama! mwana-simba mwenye manyoya shingoni akamngurumia alipokutana naye. **6** Ndipo roho ya Yehova ikaanza kutenda kazi juu yake,[m] naye akampasua vipande viwili, kama vile mtu anavyompasua mwana-mbuzi vipande viwili, wala hapakuwa na kitu chochote mkononi mwake. Naye hakumwambia baba yake wala mama yake jambo alilokuwa amefanya. **7** Naye akaendelea kushuka, akaanza kusema na yule mwanamke; na huyo mwanamke alikuwa bado ni mwenye kustahili machoni pa Samsoni.[a]

8 Basi baada ya muda akarudi kumchukua mwanamke yule nyumbani kwake.[b] Naye akageuka kando kuuangalia ule mzoga wa simba, na tazama, kulikuwa na bumba la nyuki ndani ya huo mzoga wa simba, na asali.[c] **9** Basi akaiparura na kuitia mkononi mwake, akaendelea kutembea, huku akila alipokuwa akitembea.[d] Alipojiunga tena na baba yake na mama yake, ndipo mara moja akawapa sehemu ya asali hiyo, nao wakaanza kula. Naye hakuwaambia kwamba aliitoa asali hiyo katika ule mzoga wa simba.

10 Na baba yake akaendelea kushuka mpaka kwa yule mwanamke, naye Samsoni akafanya karamu huko;[e] kwa maana hivyo ndivyo vijana walivyokuwa na desturi ya kufanya. **11** Na ikawa kwamba, walipomwona, bila kukawia wakachukua rafiki 30 za bwana-arusi, ili wakae naye. **12** Ndipo Samsoni akawaambia: "Tafadhali, acheni niwategee kitendawili.[f] Mkiniambia kwa hakika kitendawili hicho kwa muda wa siku saba[g] za karamu hii, nanyi mkitegue, ndipo nitakapowapa mavazi 30 ya ndani na nguo 30.[h] **13** Lakini mkishindwa kuniambia kitendawili hicho, ninyi mtanipa mavazi 30 ya ndani na nguo 30." Kwa hiyo wakamwambia: "Tega kitendawili chako, tukisikie."
14 Hivyo akawaambia:

"Katika mwenye kula[i]
kilitoka kitu fulani cha
kula,

SURA 13
a 1Sa 3:19
Lu 1:80
Lu 2:52
b Amu 3:10
Amu 6:34
Amu 11:29
1Sa 11:6
Mt 4:1
c Amu 18:12
d Amu 18:11
e Yos 15:33

SURA 14
f Yos 15:10
Yos 19:43
g Mwa 21:21
Mwa 34:4
Mwa 38:6
h Kut 34:16
Kum 7:3
Ne 13:27
1Ko 7:39
i Mwa 34:14
1Sa 14:6
1Sa 17:26
1Sa 31:4
2Sa 1:20
j Yos 11:20
1Fa 12:15
k Kum 28:48
Amu 13:1
Amu 15:11
l Amu 14:1
m Amu 13:25
Zek 4:6

Safu ya 2
a Amu 14:2
b Mwa 24:67
Mt 1:24
c Mwa 43:11
Kut 3:8
Kum 32:13
Met 24:13
Mt 3:4
d 1Sa 14:27
Met 25:16
e Mwa 29:22
Mt 22:4
f Zb 49:4
Zb 78:2
Met 1:6
Eze 17:2
g Mwa 29:27
h Mwa 45:22
Amu 14:19
2Fa 5:5
2Fa 5:22
i Amu 14:8

Na katika mwenye nguvu
kilitoka kitu fulani
kitamu."[a]

Nao hawakuweza kukitegua kitendawili hicho kwa muda wa siku tatu. **15** Na ikawa kwamba, katika siku ya nne wakaanza kumwambia mke wa Samsoni: "Mdanganye mume wako ili atutegulie kitendawili hicho.[b] Kama sivyo tutakuteketeza kwa moto[c] wewe na nyumba ya baba yako. Je, mlitualika hapa ili mchukue mali zetu?"[d] **16** Basi mke wa Samsoni akaanza kumlilia[e] na kusema: "Wewe unanichukia tu, unanichukia, wala hunipendi.[f] Kuna kitendawili ambacho uliwategea wana wa watu wangu,[g] lakini mimi hukuniambia." Ndipo akamwambia: "Angalia, hata sikumwambia baba yangu wala mama yangu,[h] nami je, nikuambie wewe?" **17** Lakini akaendelea kumlilia zile siku saba ambazo waliendelea na karamu, basi mwishowe ikawa kwenye siku ya saba akamwambia, kwa sababu mwanamke huyo alikuwa amemkaza.[i] Kwa hiyo mwanamke huyo akawaambia wana wa watu wake kitendawili hicho.[j] **18** Basi watu wa jiji wakamwambia siku ya saba kabla hajaenda katika chumba cha ndani:[k]

"Ni nini kilicho kitamu
kuliko asali,
Na ni nini kilicho na nguvu
kuliko simba?"[l]

Ndipo naye akawaambia:

"Kama hamngelima
na ng'ombe wangu
mchanga,[m]
Hamngekitegua
kitendawili changu."[n]

19 Halafu roho ya Yehova ikaanza kutenda kazi juu yake,[o] kisha akashuka Ashkelo-

SURA 14
a Amu 14:9
b Amu 16:5
c Amu 12:1
Amu 15:6
d Met 28:20
e Met 27:15
f Amu 16:15
g Amu 14:14
h Amu 14:9
i Amu 16:16
Met 19:13
Met 21:19
Lu 11:8
j Amu 16:18
Met 6:18
Met 25:9
k Amu 15:1
l Amu 14:14
m Amu 14:15
n Amu 14:14
o Amu 13:25
Amu 14:6
Amu 15:14
1Ko 12:4

Safu ya 2
a Yos 13:3
Amu 1:18
Yer 47:5
b Amu 14:13
c Amu 14:2
d Amu 14:11
Amu 15:2

SURA 15
e Mwa 38:17
1Sa 16:20
Lu 15:29
f Amu 14:18
g Amu 14:17
h Amu 14:11
Amu 14:20
i Amu 14:4
Amu 15:5
j Wim 2:15
Omb 5:18
k 2Sa 14:30

ni,[a] akawapiga watu 30 kati yao, akachukua mavazi aliyowavua, akawapa mavazi hayo wale wasemaji wa kile kitendawili.[b] Na hasira yake ikaendelea kuwaka, akapanda kwenda zake kwa nyumba ya baba yake.

20 Na mke wa Samsoni[c] akaja kuwa mke wa mmoja wa rafiki[d] zake aliyekuwa ameshirikiana naye.

15 Na ikawa kwamba baada ya muda, katika siku za mavuno ya ngano, Samsoni akaenda kumtembelea mke wake akiwa na mwana-mbuzi.[e] Basi akasema: "Nitaingia kwa mke wangu katika chumba cha ndani."[f] Na baba ya mwanamke huyo hakumruhusu kuingia. **2** Lakini baba yake akasema: "Kwa kweli nilisema moyoni mwangu, 'Bila shaka unamchukia.'[g] Kwa hiyo nikampa rafiki yako mwanamke huyo.[h] Je, dada yake mdogo si bora kuliko yeye? Tafadhali, yeye na awe wako badala ya yule mwingine." **3** Hata hivyo, Samsoni akawaambia: "Wakati huu sitakuwa na hatia yoyote juu ya Wafilisti nikiwadhuru."[i]

4 Na Samsoni akaondoka, akaenda zake, akawakamata mbweha[j] mia tatu, akachukua mienge na kuwageuza mkia kwa mkia na kuweka mwenge mmoja kati ya mikia miwili, katikati kabisa. **5** Ndipo akaiwasha moto ile mienge na kuwapeleka mbweha hao katika mashamba ya Wafilisti ya nafaka inayosimama. Basi akawasha moto kila kitu kuanzia mganda mpaka nafaka inayosimama na mashamba ya mizabibu na mashamba ya mizeituni.[k]

6 Na Wafilisti wakaanza kusema: "Ni nani aliyefanya jambo hili?" Ndipo wakasema: "Ni

Samsoni mwana-mkwe wa yule Mtimna, kwa sababu alimchukua mke wake, akampa rafiki yake."[a] Kwa hiyo Wafilisti wakaenda na kumteketeza kwa moto mwanamke huyo na baba yake.[b] **7** Kisha Samsoni akawaambia: "Mkifanya hivi, sina jambo lingine isipokuwa kujilipiza kisasi juu yenu,[c] kisha nitaachia hapo." **8** Naye akawapiga, akirundika miguu juu ya mapaja kwa mauaji makubwa, kisha akashuka, akaanza kukaa katika mpasuko wa mwamba Etamu.[d]

9 Baadaye Wafilisti[e] wakapanda na kupiga kambi katika Yuda,[f] wakaanza kutembea huku na huku katika Lehi.[g] **10** Ndipo watu wa Yuda wakasema: "Kwa nini mmekuja juu yetu?" nao wakasema: "Tumekuja kumfunga Samsoni, tumtendee kama vile alivyotutendea." **11** Basi watu elfu tatu wa Yuda wakashuka kwenye mpasuko wa mwamba Etamu,[h] wakamwambia Samsoni: "Je, hujui kwamba Wafilisti wanatutawala?[i] Basi jambo hili ambalo umetutendea linamaanisha nini?" Ndipo akawaambia: "Nimewatendea wao kama walivyonitendea mimi."[j] **12** Lakini wakamwambia: "Tumeshuka kuja kukufunga, tukutie mkononi mwa Wafilisti." Kwa hiyo Samsoni akawaambia: "Niapieni kwamba ninyi wenyewe hamtanishambulia." **13** Nao wakamwambia: "Hapana, tutakufunga tu, na kukutia mkononi mwao; lakini hakika hatutakuua."

Basi wakamfunga kwa kamba mbili mpya,[k] wakamtoa nje ya ule mwamba. **14** Naye akaja mpaka Lehi, nao Wafilisti wakapaaza sauti kwa shangwe walipokutana naye.[a] Na roho ya Yehova[b] ikaanza kutenda kazi juu yake, na zile kamba zilizokuwa kwenye mikono yake zikawa kama nyuzi za kitani ambazo zimeunguzwa kwa moto,[c] nazo pingu zake zikayeyuka kutoka kwenye mikono yake. **15** Akaona mfupa mbichi wa taya ya punda-dume, akanyoosha mkono wake akauchukua, akapiga nao watu elfu moja.[d] **16** Ndipo Samsoni akasema:

"Kwa mfupa wa taya
ya punda-dume—fungu
moja, mafungu mawili!
Kwa mfupa wa taya
ya punda-dume nimepiga
watu elfu moja."[e]

17 Na ikawa kwamba, alipomaliza kusema, bila kukawia akautupa ule mfupa kutoka mkononi mwake, akaita mahali hapo Ramath-lehi.[f] **18** Kisha akawa na kiu sana, na kuanza kumwita Yehova, akisema: "Wewe ndiye uliyetia wokovu huu mkubwa mkononi mwa mtumishi wako,[g] na je, sasa nife kutokana na kiu, na je, nianguke mkononi mwa wasiotahiriwa?"[h] **19** Kwa hiyo Mungu akapasua shimo lenye umbo la kinu lililokuwa katika Lehi, na maji[i] yakaanza kutoka ndani yake, naye akanywa, kisha roho[j] yake ikarudi na nguvu zikamrudia.[k] Ndiyo sababu alilita kwa jina la En-hakore, nalo lipo katika Lehi mpaka leo hii.

20 Naye akaendelea kuhukumu Israeli katika siku za Wafilisti kwa miaka 20.[l]

16 Wakati mmoja Samsoni alienda Gaza,[m] akaona mwanamke kahaba huko, akaingia kwake.[n] **2** Na Wagaza wakapewa habari, kusema: "Samsoni ameingia hapa." Basi

SURA 15

a Amu 14:11
Amu 14:20
Amu 15:2
b Kum 9:5
Amu 12:1
Amu 14:15
Met 22:8
c Mwa 9:6
Hes 35:16
Amu 14:4
d Amu 15:11
e Yos 13:2
Amu 14:4
f Yos 15:20
g Amu 15:17
Amu 15:19
2Sa 23:11
h Amu 15:8
i Kum 28:48
Amu 13:1
Amu 14:4
Zb 106:41
j Law 24:17
Amu 1:7
Amu 15:7
k Amu 16:11

Safu ya 2

a Mhu 7:8
Mik 7:8
b Amu 13:25
Amu 14:6
Zek 4:6
c Amu 16:9
Amu 16:12
d Law 26:8
Yos 23:10
1Sa 14:6
e Amu 16:30
f Amu 15:9
g Zb 3:7
Zb 18:31
Zb 44:3
h Amu 14:3
1Sa 17:26
2Sa 1:20
i Mwa 21:19
Kut 17:6
Mt 19:26
j Mwa 45:27
1Sa 30:12
Isa 40:29
k Zb 34:6
Zb 120:1
l Mwa 49:16
Amu 2:16
Amu 13:1
Amu 13:5
Amu 16:31
Ne 9:27
Ebr 11:32

SURA 16

m Yos 13:3
Yos 15:47
n Yos 2:1
Amu 14:4

wakamzunguka[a] na kumvizia
usiku kucha katika lango la jiji.[b]
Nao wakakaa kimya usiku wote,
wakisema: "Mara kutakapopa-
mbazuka asubuhi, tutamuua."[c]
3 Hata hivyo, Samsoni aka-
endelea kulala mpaka katika-
ti ya usiku, kisha akaamka ka-
tikati ya usiku, akakamata mi-
lango ya lango[d] la jiji na miimo
yake miwili, akaing'oa pamoja
na pingo, akaiweka juu ya ma-
bega yake, akaichukua[e] mpaka
kwenye kilele cha mlima ulio
mbele ya Hebroni.[f]
4 Na ikawa kwamba baada
ya hayo akampenda mwanamke
mmoja katika bonde la mto la
Soreki, na jina lake lilikuwa De-
lila.[g] **5** Ndipo wakuu wa muu-
ngano wa Wafilisti[h] wakamfikia
mwanamke huyo na kumwa-
mbia: "Mdanganye[i] ili uone ngu-
vu zake nyingi zinatokana na
nini, na kile tunachoweza kutu-
mia ili kumshinda, na kile tu-
nachoweza kutumia kumfunga
ili kumtawala; nasi tutakupa
kila mmoja wetu vipande elfu
moja na mia moja vya fedha."[j]
6 Baadaye Delila akamwa-
mbia Samsoni: "Tafadhali ni-
ambie, Hizi nguvu zako nyingi
zinatokana na nini, nawe una-
weza kufungwa kwa kitu gani
ili mtu akutawale?"[k] **7** Ndi-
po Samsoni akamwambia: "Wa-
kinifunga kwa kamba mbichi
saba za kano,[l] ambazo hazija-
kaushwa, ndipo nitakuwa dhai-
fu na kuwa kama mwanadamu
wa kawaida." **8** Basi wakuu
wa muungano wa Wafilisti[m] wa-
kamletea mwanamke huyo ka-
mba mbichi saba ambazo ha-
zijakaushwa. Baadaye akamfu-
nga kwa kamba hizo. **9** Na
watu wenye kuvizia walikuwa
wameketi katika chumba cha
ndani cha mwanamke huyo,[n]

SURA 16
a Zb 118:11
b Mdo 9:24
2Ko 11:32
c Amu 15:10
d Mwa 22:17
Mwa 24:60
e Zek 4:6
f Mwa 23:2
Yos 15:13
Yos 21:11
Amu 1:10
g Amu 16:18
h Yos 13:3
Amu 3:3
i Amu 14:15
j Kut 23:8
Hes 22:17
Amu 16:18
Met 17:23
Mhu 7:7
Mt 26:15
1Ti 6:10
k Zb 12:2
Mik 7:5
l Mwa 32:32
Ayu 10:11
m Yos 13:3
n Amu 16:12

Safu ya 2
a Yos 13:1
Yos 13:2
Amu 14:4
b Amu 15:14
c Amu 16:5
d Amu 16:4
e Amu 16:7
Amu 16:13
Amu 16:15
f Amu 16:9
g Amu 15:14
h Amu 16:7
Amu 16:11
i Amu 16:5
j Law 13:48
k Amu 16:9
l Amu 14:16
m Amu 16:7
Amu 16:11
Amu 16:13

naye akaanza kumwambia:
"Wafilisti[a] wako juu yako, Sa-
msoni!" Ndipo akazikata kamba
hizo vipande viwili, kama vile
nyuzi za kitani zilizosokotwa
zinavyokatika vipande viwili
zinaponusa harufu ya moto.[b] Na
nguvu zake hazikujulikana.[c]
10 Basi Delila[d] akamwambia
Samsoni: "Tazama! Umeniche-
zea, ukaniambia uwongo.[e] Sasa
niambie tafadhali, unaweza ku-
fungwa na kitu gani." **11** Kwa
hiyo akamwambia: "Wakinifu-
nga kwa kamba mpya ambazo
hazijafanyiwa kazi yoyote, nita-
kuwa dhaifu na kuwa kama
mwanadamu wa kawaida."
12 Basi Delila akachukua ka-
mba mpya akamfunga nazo,
akamwambia: "Wafilisti wako
juu yako, Samsoni!" Wakati huo
wote wale watu wenye kuvi-
zia walikuwa wameketi kati-
ka chumba cha ndani.[f] Ndipo
akazikata vipande viwili kutoka
mikononi mwake kama uzi.[g]
13 Kisha Delila akamwa-
mbia Samsoni: "Mpaka sasa
umenichezea, ukaniambia uwo-
ngo.[h] Niambie unaweza kufu-
ngwa na kitu gani."[i] Ndipo aka-
mwambia: "Ukifuma hii misu-
ko saba ya nywele za kichwa
changu kwa uzi wa mtande."[j]
14 Basi akazikaza kwa msuma-
ri, kisha akamwambia: "Wafili-
sti wako juu yako, Samsoni!"[k]
Ndipo akaamka kutoka kati-
ka usingizi wake, akaung'oa ule
msumari wa wafumaji na ule uzi
wa mtande.
15 Mwanamke akamwambia:
"Unawezaje kuthubutu kusema,
'Nakupenda,'[l] ingawa moyo wako
haupo pamoja nami? Umeniche-
zea mara tatu hizi nawe hu-
janiambia nguvu zako zinato-
kana na nini."[m] **16** Na ikawa
kwamba kwa sababu mwanamke

huyo alimkaza[a] kwa maneno
yake wakati wote na kuende-
lea kumsihi, nafsi yake ikako-
sa subira kufikia hatua ya kuta-
ka kufa.[b] **17** Mwishowe aka-
mfunulia moyo wake[c] wote na
kumwambia: "Wembe[d] haujapi-
ta kamwe juu ya kichwa cha-
ngu, kwa kuwa mimi ni Mna-
dhiri wa Mungu tangu tumboni
mwa mama yangu.[e] Nikinyole-
wa, hakika nguvu zangu zita-
nitoka, nami hakika nitakuwa
dhaifu na kuwa kama wanada-
mu wengine wote."[f]
18 Delila alipoona kwamba
amemfunulia moyo wake wote,
akapeleka neno haraka na ku-
waita wakuu wa muungano wa
Wafilisti,[g] akisema: "Njooni sa-
fari hii, kwa maana amenifunu-
lia moyo wake wote."[h] Na wa-
kuu wa muungano wa Wafi-
listi wakamfikia huyo mwana-
mke ili walete zile pesa
mkononi mwao.[i] **19** Na ndi-
po huyo mwanamke akamlaza
magotini pake. Akamwita mtu
akamnyoa ile misuko saba ya
nywele za kichwa chake, kisha
mwanamke huyo akaanza ku-
mtawala, na nguvu zake zikaen-
delea kumtoka. **20** Basi aka-
sema: "Wafilisti wako juu yako,
Samsoni!" Naye akaamka ku-
toka katika usingizi na kuse-
ma: "Nitatoka nje kama safari
zile nyingine[j] na kujitikisa niwe
huru." Naye hakujua kwamba
Yehova alikuwa amemwacha.[k]
21 Basi Wafilisti wakamkama-
ta, wakayang'oa macho[l] yake
na kumshusha mpaka Gaza,[m]
wakamfunga kwa pingu mbi-
li za shaba;[n] naye akawa mtu
mwenye kusaga[o] katika nyu-
mba ya gereza.[p] **22** Wakati
huo nywele za kichwa chake zi-
kaanza kukua sana mara baada
ya kunyolewa.[q]

SURA 16

a Amu 14:17
Lu 11:8
b Met 21:19
Met 25:24
Met 27:15
Lu 11:8
c Amu 14:17
Mik 7:5
d Hes 6:5
Amu 13:5
1Sa 1:11
e Amu 13:7
f Met 13:3
g Yos 13:3
Amu 3:3
Amu 16:5
Amu 16:30
1Sa 5:8
1Sa 6:4
1Sa 29:2
1Nya 12:19
h Amu 14:17
Amu 16:17
Met 25:9
Yer 9:4
Mik 7:5
i Amu 16:5
Mt 26:15
j Amu 16:9
Amu 16:12
Amu 16:14
k Hes 14:42
1Sa 18:12
2Nya 15:2
l 1Sa 11:2
2Fa 25:7
m Amu 16:1
n 2Nya 33:11
o Mk 9:42
p Mwa 39:20
2Fa 17:4
q Hes 6:5
Amu 13:5

Safu ya 2

a 1Sa 5:4
b Kum 32:27
Amu 13:5
c Zb 135:15
Da 5:4
1Ko 8:5
d Amu 15:10
e Amu 15:5
f Amu 15:8
Amu 15:16
g 2Sa 13:28
h Met 14:13
Mt 27:29
i Ayu 30:9
Zb 35:15
Zb 69:12
Ebr 11:36
j Amu 16:18
k Amu 16:25
l Ebr 11:32
m Zb 50:15
Zb 91:15
n Zb 74:18
Yer 15:15
o Amu 14:6
Amu 14:19
Amu 15:14
p Amu 16:21
Zb 58:10
Zb 143:12

23 Lakini wale wakuu wa
muungano wa Wafilisti wakaku-
sanyika pamoja ili kutoa dhabi-
hu kubwa kwa Dagoni[a] mu-
ngu wao na ili washangilie,
nao wakawa wakisema: "Mu-
ngu wetu amemtia mkononi
mwetu Samsoni adui yetu!"[b]
24 Na watu walipomwona,
mara moja wakaanza kumsifu
mungu wao,[c] "kwa sababu," wa-
kasema, "mungu wetu amemtia
katika mkono wetu adui yetu[d]
na mwenye kuharibu nchi yetu[e]
na mtu aliyezidisha hesabu ya
watu wetu waliouawa."[f]
25 Na ikawa kwamba kwa
kuwa moyo wao ulikuwa na fu-
raha,[g] wakaanza kusema: "Mwi-
te Samsoni apate kututumbui-
za."[h] Basi wakamwita Samso-
ni kutoka katika ile nyumba
ya gereza apate kucheza mbele
yao;[i] nao wakamsimamisha ka-
tikati ya nguzo. **26** Ndipo Sa-
msoni akamwambia yule mvu-
lana aliyekuwa amemshika
mkono: "Niruhusu niguse ngu-
zo ambazo nyumba imesimami-
shwa imara juu yake, nami ni-
ziegemee." **27** (Basi nyumba
hiyo ilikuwa imejaa wanaume
na wanawake na wakuu wote
wa muungano wa Wafilisti wali-
kuwa humo;[j] na juu ya dari wa-
likuwapo karibu watu elfu tatu,
wanaume na wanawake, walio-
kuwa wakitazama huku Samso-
ni akitumbuiza.)[k]
28 Sasa Samsoni[l] akamwi-
ta Yehova[m] na kusema: "Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova,
tafadhali nikumbuke,[n] tafadha-
li unitie nguvu,[o] mara hii moja
tu, Ee Mungu wa kweli, ili nji-
lipize kisasi juu ya Wafilisti kwa
ajili ya jicho langu moja kati ya
macho yangu mawili."[p]
29 Ndipo Samsoni akajiina-
misha kwa zile nguzo mbili za

katikati ambazo juu yake nyumba ilikuwa imesimamishwa imara, naye akazishika, moja kwa mkono wake wa kuume na ile nyingine kwa mkono wake wa kushoto. **30** Kisha Samsoni akasema: "Nafsi yangu na ife[a] pamoja na Wafilisti." Ndipo akajiinamisha kwa nguvu, na nyumba ile ikawaangukia wale wakuu wa muungano na watu wote waliokuwamo ndani,[b] hivi kwamba wafu alioua wakati wa kifo chake wakawa wengi kuliko wale alioua wakati wa maisha yake.[c]

31 Baadaye ndugu zake na nyumba yote ya baba yake wakashuka, wakamwinua, wakamleta na kumzika kati ya Sora[d] na Eshtaoli[e] katika kaburi la Manoa[f] baba yake. Naye alikuwa amehukumu Israeli kwa miaka 20.[g]

17 Basi palikuwa na mwanamume kutoka katika eneo lenye milima la Efraimu[h] ambaye jina lake lilikuwa Mika. **2** Baada ya muda akamwambia mama yake: "Vile vipande elfu moja na mia moja vya fedha vilivyochukuliwa kutoka kwako na ambavyo ulitoa laana[i] juu yake na pia ukasema masikioni mwangu—tazama! mimi nina fedha hizo. Mimi ndiye niliyezichukua."[j] Ndipo mama yake akasema: "Mwanangu na awe mbarikiwa wa Yehova."[k] **3** Basi akamrudishia mama yake[l] vile vipande elfu moja na mia moja vya fedha; naye mama yake akaendelea kusema: "Bila shaka nitazitakasa fedha hizi kwa Yehova kutoka mkononi mwangu kwa ajili ya mwanangu, ili kutengeneza sanamu ya kuchongwa[m] na sanamu ya kuyeyushwa;[n] na sasa nitairudisha kwako."

SURA 16

a Eze 18:4
Mt 10:28
Ufu 12:11
b Amu 16:27
Ayu 31:3
c Amu 14:19
Amu 15:8
Amu 15:15
d Amu 13:2
Amu 13:25
e Yos 19:41
f Amu 13:8
g Mwa 49:16
Amu 2:16
Amu 15:20

SURA 17

h Yos 17:15
Amu 10:1
i 1Sa 14:24
1Sa 26:19
j Kut 20:12
Kut 20:15
Law 6:4
k Met 19:18
l Law 6:4
m Kut 20:4
Law 26:1
Zb 115:4
n Law 19:4
Isa 40:19
Hab 2:18

Safu ya 2

a Isa 46:6
Yer 10:9
b Kum 5:8
Kum 27:15
c Kum 9:12
d Mwa 31:30
Kum 13:6
Ezr 1:7
1Ko 8:5
e Kut 28:6
Amu 8:27
f Mwa 31:19
Amu 18:14
Ho 3:4
g Kut 29:9
Amu 17:12
1Fa 13:33
2Nya 13:9
h Hes 3:10
Kum 12:11
i Mwa 36:31
Kum 33:5
Amu 18:1
j Kum 12:8
Kum 28:1
Amu 21:25
Met 14:12
Met 16:2
Met 21:2
k Mwa 35:19
Amu 19:1
Ru 1:1
Mik 5:2
Mt 2:1
l Hes 3:45
Yos 14:3
Yos 18:7
Amu 18:30
m Amu 17:1
n Mwa 45:8
2Fa 6:21
Isa 22:21
o Amu 18:19
Amu 18:27
p Amu 17:5

4 Basi akamrudishia mama yake fedha hizo, kisha mama yake akachukua vipande mia mbili vya fedha akampa fundi wa fedha.[a] Naye akatengeneza sanamu ya kuchongwa[b] na sanamu ya kuyeyushwa;[c] nayo ikawa katika nyumba ya Mika. **5** Na mtu huyo Mika, alikuwa na nyumba ya miungu,[d] naye akafanya efodi[e] na terafimu,[f] akaujaza nguvu mkono[g] wa mmoja wa wanawe, ili awe kuhani[h] wake. **6** Siku hizo hapakuwa na mfalme katika Israeli.[i] Kila mtu alikuwa akifanya yaliyo sawa machoni pake mwenyewe kulingana na alivyozoea kufanya.[j]

7 Basi palikuwa na kijana wa Bethlehemu[k] katika Yuda wa familia ya Yuda, naye alikuwa Mlawi.[l] Alikuwa anakaa hapo kwa muda. **8** Na mtu huyo akaondoka jiji la Bethlehemu katika Yuda ili akae kwa muda mahali popote ambapo angepata makao. Baadaye alipokuwa akienda zake akaja katika eneo lenye milima la Efraimu mpaka kwenye nyumba ya Mika.[m] **9** Ndipo Mika akamwambia: "Unatoka wapi?" Naye akamjibu: "Mimi ni Mlawi kutoka Bethlehemu katika Yuda, nami niko njiani ili nikakae kwa muda mahali popote nitakapopata makao." **10** Basi Mika akamwambia: "Kaa pamoja na mimi, uwe kama baba[n] na kuhani[o] kwangu, nami nitakupa vipande kumi vya fedha kwa mwaka na mavazi ya kawaida na chakula chako." Ndipo Mlawi huyo akaingia ndani. **11** Basi Mlawi huyo akajiamulia mwenyewe kukaa pamoja na mtu yule, na huyo kijana akawa kama mmoja wa wanawe. **12** Na zaidi, Mika akaujaza nguvu mkono[p]

wa huyo Mlawi, ili huyo kijana awe kuhani[a] kwake na apate kuendelea kuishi katika nyumba ya Mika. **13** Basi Mika akasema: "Sasa najua kwamba Yehova atanitendea mema, kwa maana Mlawi amekuwa kuhani kwangu."[b]

18 Siku hizo hapakuwa na mfalme katika Israeli.[c] Na katika siku hizo kabila la Wadani[d] walikuwa wakijitafutia urithi ili wakae humo; kwa sababu kufikia wakati huo, urithi haukuwa umewaangukia katikati ya makabila ya Israeli.[e]

2 Mwishowe wana wa Dani wakatuma watu watano wa familia yao, wanaume kutoka kati yao, wanaume waliokuwa watu mashujaa, kutoka katika Sora[f] na Eshtaoli,[g] wapate kuipeleleza[h] nchi na kuichunguza. Basi wakawaambia: "Nendeni, chunguzeni nchi." Baadaye wakaja katika eneo lenye milima la Efraimu[i] mpaka kwenye nyumba ya Mika,[j] wakalala hapo usiku kucha. **3** Walipokuwa karibu na nyumba ya Mika, wakatambua sauti ya yule kijana, Mlawi, kisha wakageuka kando kuingia humo. Nao wakamwambia: "Ni nani aliyekuleta hapa, nawe unafanya nini hapa, nawe una shughuli gani hapa?" **4** Naye akawaambia: "Mika alinitendea hivi na hivi ili anikodishe,[k] na ili niwe kuhani[l] kwake." **5** Ndipo wakamwambia: "Tafadhali, uliza[m] kutoka kwa Mungu[n] ili tupate kujua kama njia yetu tunayoiendea itafanikiwa." **6** Basi kuhani huyo akawaambia: "Nendeni kwa amani. Njia yenu mnayoiendea iko mbele za Yehova."

7 Basi hao watu watano wakaendelea, wakaja Laishi,[o] wakaona jinsi ambavyo watu wa-

SURA 17

a Hes 3:10
1Fa 12:31
1Fa 13:33
2Nya 13:9
b Met 14:12
Isa 44:20
Mt 15:9

SURA 18

c Mwa 36:31
Kum 33:5
Amu 8:23
Amu 17:6
Amu 19:1
Amu 21:25
d Yos 19:40
e Hes 33:55
Yos 19:47
Amu 1:34
f Yos 19:41
Amu 13:2
Amu 13:25
g Amu 16:31
h Hes 13:17
Yos 2:1
Yos 7:2
Amu 1:23
1Sa 26:4
i Yos 17:15
Amu 19:1
j Amu 17:1
k Amu 17:10
Mik 3:11
l Amu 17:5
Amu 18:27
1Fa 13:33
2Nya 13:9
m 1Fa 22:5
n Amu 17:13
o Yos 19:47
Amu 18:29

Safu ya 2

a Amu 18:27
b Yos 13:4
Yos 19:28
Amu 3:3
Amu 10:12
c Amu 13:2
Amu 16:31
d Yos 15:33
Amu 18:2
e Hes 14:7
Kum 8:7
f Kut 23:30
Hes 13:30
Yos 18:3
g Amu 18:7
Amu 18:27
h Kum 4:1
Zb 81:14
i Kut 3:8
Kum 8:9
Eze 20:6
j Yos 19:40
k Amu 16:31
Amu 18:2
l Yos 15:60
1Sa 7:1
2Nya 1:4
m Amu 13:25
n Amu 17:1
o Amu 18:2
p Amu 18:7
Amu 18:29
q Amu 17:5
r Kum 5:8
Amu 17:4

liokuwa humo walikaa kwa kujitegemea kulingana na desturi ya Wasidoni, watulivu na wasio na shaka,[a] wala hapakuwa na mshindi mwenye kukandamiza aliyekuwa akileta usumbufu wowote katika nchi, nao walikuwa mbali sana na Wasidoni,[b] wala hawakuwa na shughuli yoyote na wanadamu.

8 Mwishowe wakaja kwa ndugu zao huko Sora[c] na Eshtaoli,[d] nao ndugu zao wakawaambia: "Haya, mna habari gani?" **9** Nao wakasema: "Simameni, nasi tupande juu yao; kwa maana tumeiona nchi, na tazama! ni nzuri sana.[e] Nanyi mnasitasita. Msiwe goigoi kuhusu kwenda kuingia kuimiliki nchi ile.[f] **10** Mtakapoingia, mtawafikia watu wasio na shaka,[g] na nchi ile ni pana sana; kwa maana Mungu ameitia mkononi mwenu,[h] mahali ambapo hakuna ukosefu wa kitu cha aina yoyote kilicho duniani."[i]

11 Ndipo watu mia sita waliojifunga silaha za vita, kutoka katika familia ya Wadani,[j] wakaondoka hapo, yaani, kutoka Sora na Eshtaoli.[k] **12** Nao wakaondoka, wakapanda, wakapiga kambi huko Kiriath-yearimu[l] katika Yuda. Ndiyo sababu wamepaita mahali hapo Mahane-dani[m] mpaka leo hii. Tazama! Pako upande wa magharibi wa Kiriath-yearimu. **13** Baadaye wakapita kutoka hapo mpaka eneo lenye milima la Efraimu, wakaja mpaka nyumba ya Mika.[n]

14 Ndipo wale watu watano waliokuwa wameenda kuipeleleza[o] nchi ya Laishi[p] wakajibu na kuwaambia ndugu zao: "Je, mlijua kwamba katika nyumba hizi mna efodi na terafimu[q] na sanamu ya kuchongwa[r] na sa-

namu ya kuyeyushwa?[a] Na sasa
mfikirie akilini yale mtakayofa-
nya."[b] **15** Basi wakageuka kan-
do hapo, wakaja katika nyu-
mba ya yule kijana, Mlawi,[c]
nyumbani kwa Mika, wakaanza
kuuliza habari[d] za hali yake.
16 Na wakati huo wale wana-
ume mia sita waliojifunga sila-
ha za vita,[e] waliokuwa ni wana
wa Dani,[f] walikuwa wamesi-
mama kwenye mwingilio wa la-
ngo. **17** Kisha wale watu wa-
tano ambao walikuwa wame-
toka kwenda kuipeleleza nchi[g]
wakapanda, ili waingie humo
ndani, waichukue ile sanamu ya
kuchongwa[h] na ile efodi[i] na ile
terafimu[j] na ile sanamu ya ku-
yeyushwa.[k] (Na yule kuhani[l] ali-
kuwa amesimama kwenye mwi-
ngilio wa lango pamoja na wale
watu mia sita waliojifunga sila-
ha za vita.) **18** Nao wakaing-
ia katika nyumba ya Mika,
wakachukua ile sanamu ya ku-
chongwa, ile efodi na ile te-
rafimu na ile sanamu ya ku-
yeyushwa.[m] Kisha yule kuha-
ni[n] akawaambia: "Mnafanya
nini?" **19** Lakini wakamwa-
mbia: "Nyamaza. Weka mkono
wako juu ya kinywa chako, na
uende pamoja nasi, uwe baba[o]
na kuhani[p] kwetu. Ni jambo
gani lililo bora, wewe uende-
lee kuwa kuhani kwa nyumba
ya mtu mmoja[q] au kuwa ku-
hani kwa kabila na familia ka-
tika Israeli?"[r] **20** Ndipo moyo
wa kuhani huyo ukafurahi,[s]
basi akachukua ile efodi na ile
terafimu na ile sanamu ya ku-
chongwa,[t] akaja katikati ya
wale watu.

21 Nao wakageuka wakaenda
zao, wakaweka watoto wadogo
na mifugo na vitu vyenye tha-
mani mbele yao.[u] **22** Waliku-
wa wameenda mwendo fulani

SURA 18

a Kum 27:15
1Yo 5:21
b Amu 18:18
c Amu 17:7
Amu 17:12
Amu 18:30
d Mwa 29:6
Mwa 43:27
e 1Sa 17:5
2Nya 26:14
f Amu 18:11
g Amu 18:2
h Kut 20:4
Law 26:1
Amu 17:4
Zb 115:4
i Kut 28:6
Amu 8:27
j Mwa 31:19
Mwa 31:30
Amu 17:5
Ho 3:4
k Law 19:4
Kum 27:15
Amu 17:3
1Yo 5:21
l Amu 17:12
m Amu 17:4
Amu 18:30
n Amu 17:12
Amu 18:4
o Amu 17:10
p Amu 18:4
Amu 18:27
Mik 3:11
q Amu 17:12
r Amu 18:30
s Zb 10:3
Isa 56:11
Ebr 5:4
t Amu 17:4
Amu 17:5
Amu 18:14
Amu 18:18
u Mwa 33:2
Kum 25:18

Safu ya 2

a Amu 17:1
b Mwa 21:17
2Sa 14:5
2Fa 6:28
c Amu 17:4
Amu 17:5
d Zb 115:8
Zb 135:18
Isa 44:17
Yer 51:17
e Amu 17:12
f Amu 17:5
g 1Sa 22:2
h Lu 14:31
i Amu 17:12
Amu 18:19
j Yos 19:47
Amu 18:7
k Amu 18:10
l Yos 19:47
m Yos 11:13
n Mwa 10:15
Mwa 49:13
Yos 11:8
Amu 10:12
Amu 18:7
o Hes 13:21
2Sa 10:6
p Hes 33:53
q Mwa 14:14
Kum 34:1
Yos 19:47
Amu 20:1
2Sa 17:11
1Fa 12:29
r Mwa 30:6
Mwa 32:28

kutoka nyumba ya Mika wa-
kati wanaume waliokuwa katika
nyumba zilizo karibu na nyu-
mba ya Mika[a] walipokusanywa
pamoja na kujaribu kuwafikia
wana wa Dani. **23** Walipozidi
kuwalilia wana wa Dani, ndipo
wakageuza nyuso zao na ku-
mwambia Mika: "Una nini
wewe,[b] hata mkakusanyika?"
24 Basi akasema: "Mmeichukua
miungu[c] ambayo nilitengene-
eza,[d] kuhani[e] pia, nanyi mnae-
nda zenu, nami nina nini tena?[f]
Basi mnawezaje kuniambia, 'Una
nini wewe?'" **25** Ndipo wana
wa Dani wakamwambia: "Usia-
che sauti yako isikike karibu
nasi, ili kwamba watu wenye
uchungu wa nafsi[g] wasije wa-
kawashambulia ninyi, nawe
upoteze nafsi yako mwenyewe
na nafsi za watu wa nyumba-
ni mwako." **26** Nao wana wa
Dani wakaendelea kwenda zao;
na Mika akaona kwamba wana
nguvu kuliko yeye,[h] basi akageu-
ka, akarudi nyumbani kwake.

27 Lakini wao walichukua
vitu ambavyo Mika alikuwa
ametengeneza na yule kuha-
ni[i] aliyekuwa wake, wakaele-
kea Laishi,[j] juu ya watu watuli-
vu na wasio na shaka.[k] Nao wa-
kaanza kuwapiga kwa makali
ya upanga,[l] wakaliteketeza jiji
kwa moto.[m] **28** Wala hapakuwa
na mkombozi, kwa maana
lilikuwa mbali sana na Sidoni,[n]
nao hawakuwa na shughuli yo-
yote kabisa na wanadamu; na
ilikuwa katika nchi tambara-
re ya chini iliyokuwa ya Beth-
rehobu.[o] Kisha wakalijenga jiji
na kuanza kukaa ndani yake.[p]
29 Zaidi ya hayo, wakaita jiji
hilo jina Dani kulingana na
jina la baba yao, Dani,[q] aliye-
zaliwa kwa Israeli.[r] Hata hi-
vyo, jina la jiji hilo hapo zamani

lilikuwa Laishi.[a] **30** Kisha
wana wa Dani wakajisimamishia ile sanamu ya kuchongwa;[b]
naye Yonathani[c] mwana wa Gershomu,[d] mwana wa Musa, yeye
na wanawe wakawa makuhani
kwa kabila la Wadani mpaka
siku ile nchi ilipopelekwa uhamishoni.[e] **31** Nao wakaendelea kujisimamishia ile sanamu
ya kuchongwa ya Mika, ambayo alikuwa ameitengeneza, siku
zote ambazo ile nyumba[f] ya Mungu wa kweli iliendelea kuwa
katika Shilo.[g]

19 Basi ikawa katika siku
hizo kwamba hapakuwa
na mfalme katika Israeli.[h] Na
ikawa kwamba Mlawi fulani alikuwa anakaa kwa muda katika sehemu za mbali zaidi za
eneo lenye milima la Efraimu.[i]
Baadaye akachukua suria[j] kutoka Bethlehemu[k] katika Yuda
awe mke wake. **2** Ndipo suria
wake akaanza kufanya uasherati[l] dhidi yake. Mwishowe suria huyo akamwacha, akaenda
nyumbani kwa baba yake huko
Bethlehemu katika Yuda, akaendelea kukaa huko miezi minne
kamili. **3** Ndipo mume wake
akasimama, akamfuata ili kuzungumza naye kwa sauti ya kufariji ili amrudishe; naye alikuwa pamoja na mtumishi[m] wake
na punda-dume wawili. Basi
mwanamke huyo akamleta katika nyumba ya baba yake. Wakati baba ya huyo mwanamke kijana alipomwona, mara moja akafurahi kuonana naye. **4** Basi
baba-mkwe wake, baba ya yule
mwanamke kijana, akamzuia,
akaendelea kukaa pamoja naye
kwa siku tatu; nao wakawa wakila na kunywa, naye akawa
akilala hapo usiku kucha.[n]

5 Na ikawa kwamba katika
siku ya nne, walipoamka asubuhi na mapema kama kawaida, akasimama ili kwenda, lakini baba ya yule mwanamke kijana akamwambia mwana-mkwe
wake: "Lisha moyo wako kipande
cha mkate,[a] kisha baadaye mwende zenu." **6** Basi wakaketi,
na wote wawili wakaanza kula
na kunywa pamoja; kisha
baba ya yule mwanamke kijana akamwambia yule mwanamume: "Kubali, tafadhali, kulala usiku kucha,[b] na acha moyo wako
uchangamke."[c] **7** Wakati huyo
mwanamume aliposimama ili aende, baba-mkwe wake akaendelea kumsihi, hivi kwamba akalala hapo tena usiku kucha.[d]

8 Alipoamka asubuhi na mapema katika siku ya tano ili aende, baba ya yule mwanamke kijana akasema: "Tafadhali, kula
kitu fulani kwa ajili ya moyo
wako."[e] Nao wakakawia mpaka mchana kutwa. Na wote wawili wakaendelea kula. **9** Ndipo yule mwanamume[f] akasimama ili aende, yeye pamoja na suria[g] wake na mtumishi[h] wake;
lakini baba-mkwe wake, baba
ya yule mwanamke kijana, akamwambia: "Tazama, sasa! Mchana umesonga kuelekea kuwa jioni. Tafadhali, laleni usiku
kucha.[i] Tazama mchana unakaribia
mwisho wake. Lala hapa usiku kucha, na acha moyo wako
uchangamke.[j] Nanyi kesho mwamke mapema kwa ajili ya safari yenu, nawe uende hemani kwako." **10** Hata hivyo, mwanamume huyo hakukubali kulala usiku
kucha, bali alisimama, akaondoka na kwenda mpaka mbele ya
Yebusi,[k] yaani, Yerusalemu;[l] naye
alikuwa na wale punda-dume wawili waliotandikwa, na suria
wake na mtumishi wake.

11 Walipokuwa karibu na
Yebusi, kwa kuwa mchana uli-

SURA 18

a Yos 19:47
Amu 18:7
b Kut 20:4
Law 26:1
Kum 17:3
Kum 27:15
Amu 17:4
Amu 18:18
c Amu 17:12
d Kut 2:22
Kut 18:3
e 1Sa 4:11
1Sa 4:22
Zb 78:61
f Kut 40:2
Yos 18:1
g 1Sa 1:3
1Sa 4:3
Zb 78:60
Yer 7:12

SURA 19

h Amu 17:6
Amu 18:1
Amu 21:25
1Sa 8:4
1Sa 8:5
i Yos 17:15
Yos 17:16
j Mwa 16:3
Kut 21:8
2Sa 5:13
2Nya 11:21
k Mwa 35:19
Amu 17:7
Mik 5:2
Mt 2:6
l Law 20:10
Kum 22:22
Ga 5:19
Kol 3:5
m Hes 22:22
n Mwa 24:54
Ro 12:13
Ebr 13:2

Safu ya 2

a Mwa 18:5
Zb 104:15
Met 11:25
b Mwa 19:2
c Amu 19:9
Amu 19:22
d Amu 19:4
1Pe 4:9
e Mwa 18:5
Amu 19:5
Ru 3:7
Zb 104:15
f Amu 19:1
g Amu 19:2
2Sa 5:13
h Hes 22:22
Amu 19:3
i Lu 24:29
Ro 12:13
j Amu 19:6
k Yos 15:8
Yos 15:63
l Yos 18:28
Amu 1:8

kuwa umeendelea sana,[a] yule
mtumishi akamwambia bwana
wake: "Haya, tafadhali, na tuge-
uke kando tuingie katika jiji hili
la Wayebusi,[b] tulale humo usi-
ku kucha." **12** Lakini bwana
wake akamwambia: "Tusigeu-
ke kando kuingia katika jiji la
wageni[c] ambao si sehemu ya
wana wa Israeli; basi tuvuke
mpaka Gibea."[d] **13** Naye aka-
mwambia tena mtumishi wake:
"Haya, na tukaribie mojawapo
ya mahali hapa, tulale usiku ku-
cha ama katika Gibea au ka-
tika Rama."[e] **14** Basi wakavu-
ka, wakazidi kwenda zao, ndipo
jua likaanza kutua juu yao wa-
lipokuwa karibu na Gibea, jiji la
Benyamini.

15 Basi wakageuka kando
hapo ili kuingia ndani walale
usiku kucha katika Gibea. Ki-
sha wakaingia na kuketi katika
kiwanja cha watu wote cha jiji,
wala hakuna yeyote aliyewaka-
ribisha ndani ya nyumba ili wa-
lale usiku kucha.[f] **16** Mwisho-
we, tazama! mwanamume fula-
ni mzee akaingia, akitoka kufa-
nya kazi yake shambani wakati
wa jioni,[g] na mtu huyo alikuwa
wa kutoka katika eneo lenye mi-
lima la Efraimu,[h] naye alikuwa
anakaa kwa muda katika Gibea;
lakini watu wa mahali hapo wa-
likuwa Wabenyamini.[i] **17** Ali-
poinua macho yake, akamwona
yule mtu, yule msafiri, katika
kiwanja cha watu wote cha jiji.
Basi huyo mwanamume mzee
akauliza: "Unaenda wapi, nawe
unatoka wapi?"[j] **18** Naye aka-
mwambia: "Tunavuka kutokea
Bethlehemu ya Yuda kwenda
katika sehemu za mbali zaidi
za eneo lenye milima la Efrai-
mu.[k] Huko ndiko ninakotoka,
lakini nilienda Bethlehemu ya
Yuda;[l] nami ninaiendea nyumba
yangu mwenyewe, wala hakuna
yeyote anayenikaribisha ndani
ya nyumba yake.[a] **19** Na kuna
majani na pia chakula cha mifu-
go[b] kwa ajili ya punda zetu, na
kuna mkate[c] na divai pia kwa
ajili yangu na kwa ajili ya kija-
kazi[d] wako na kwa ajili ya mtu-
mishi[e] aliye pamoja na mtumi-
shi wako. Hakuna ukosefu wa
hata kitu kimoja." **20** Hata hi-
vyo, yule mzee akasema: "Uwe
na amani![f] Upungufu wowote
upande wako na uwe juu ya-
ngu.[g] Lakini usilale usiku kucha
katika kiwanja cha watu wote."
21 Ndipo akamwingiza ndani
ya nyumba yake,[h] akawatupia
wale punda chakula cha mcha-
nganyiko.[i] Kisha wakaosha mi-
guu yao,[j] wakaanza kula na ku-
nywa.

22 Walipokuwa wakichanga-
msha mioyo yao,[k] tazama! wa-
naume wa jiji lile, watu wasi-
ofaa kitu,[l] wakaizunguka nyu-
mba,[m] wakisukumana mlango-
ni; nao wakazidi kumwambia
yule mzee, mwenye nyumba:
"Mtoe nje yule mwanamume
aliyeingia nyumbani mwako, ili
tulale naye."[n] **23** Ndipo mwe-
nye nyumba akatoka nje, aka-
waendea na kuwaambia:[o] "Ha-
pana, ndugu zangu,[p] tafadhali
msifanye jambo lolote baya,
kwa kuwa mtu huyu ameingia
nyumbani mwangu. Msitende
upumbavu huu wenye kufedhe-
hesha.[q] **24** Hapa pana binti
yangu aliye bikira na suria wa
mtu huyu. Tafadhali, acheni ni-
walete nje, nanyi mpate kuwa-
lala kinguvu[r] na kuwatendea
yaliyo mema machoni penu. La-
kini msimtendee mwanamume
huyu jambo hili la upumbavu na
lenye kufedhehesha."

25 Lakini wanaume hao ha-
wakutaka kumsikiliza. Basi

SURA 19

a Amu 19:14
b Mwa 10:16
c Kut 23:33
Hes 33:55
Kum 20:18
Amu 1:21
d Yos 18:28
1Sa 10:26
Isa 10:29
Ho 5:8
e Yos 18:25
1Fa 15:17
Ne 11:33
Yer 40:1
f Mwa 19:2
Amu 19:20
Isa 58:7
g Mt 20:8
h Yos 17:15
Amu 19:1
i Yos 18:21
Yos 18:28
j Mwa 16:8
k Amu 19:1
l Amu 19:2

Safu ya 2

a Amu 19:15
b Mwa 24:32
Mwa 43:24
c Mwa 18:5
d Amu 19:2
e Amu 19:3
Amu 19:9
f Amu 6:23
1Sa 25:6
1Nya 12:18
g Amu 19:15
Ro 12:13
Ebr 13:2
1Pe 4:9
h Mwa 19:3
Mdo 16:15
i Amu 19:19
j Mwa 18:4
1Sa 25:41
2Sa 11:8
Lu 7:44
Yoh 13:5
1Ti 5:10
k Amu 19:6
Amu 19:9
Zb 104:15
l Kum 13:13
Amu 20:13
Met 6:12
Met 16:27
Nah 1:15
m Mwa 19:4
Amu 20:5
n Mwa 19:5
Law 20:13
Ro 1:27
1Ko 6:9
Yud 7
o Mwa 19:6
p Mwa 19:7
q Mwa 34:7
Amu 20:6
r Mwa 19:8

mtu huyo akamchukua suria[a]
wake na kumleta kwao nje;
nao wakaanza kulala na mwa-
namke huyo,[b] wakaendelea ku-
mtendea vibaya[c] usiku wote
mpaka asubuhi, kisha waka-
mwacha aende wakati wa ma-
pambazuko. **26** Ndipo mwa-
namke huyo akaja asubuhi ili-
pokuwa ikikaribia, akaanguka
mlangoni pa nyumba ya yule
mtu ambapo bwana wake ali-
kuwa,[d]—mpaka wakati wa ma-
pambazuko. **27** Baadaye bwa-
na wake akaamka asubuhi, aka-
fungua milango ya nyumba,
akatoka nje kwenda zake, na
tazama! yule mwanamke, suria
wake,[e] ameanguka kwenye mla-
ngo wa nyumba, mikono yake
ikiwa juu ya kizingiti! **28** Basi
akamwambia: "Simama, twe-
nde." Lakini hakuna aliyejibu.[f]
Kwa hiyo mwanamume huyo
akamchukua juu ya punda, aka-
ondoka, akaenda kwake.[g]

29 Ndipo akaingia ndani ya
nyumba yake, akachukua kisu
cha kuchinjia, akamshika yule
suria wake, akamkatakata vi-
pande kwa kufuatisha mifupa
yake, vipande kumi na viwili[h]
naye akampeleka katika kila
eneo la Israeli.[i] **30** Na ikatu-
kia kwamba kila mtu aliyeo-
na jambo hilo akasema: "Jambo
kama hili halijawahi kutokea
kamwe wala kuonekana tangu
siku wana wa Israeli walipopa-
nda kutoka nchi ya Misri mpa-
ka leo. Wekeni jambo hili mio-
yoni mwenu, fanyeni shauri[j] na
mseme."

20 Basi wana wote wa Isra-
eli wakatoka,[k] na kusa-
nyiko likakutanika kama mtu
mmoja,[l] kutoka Dani[m] mpaka
Beer-sheba[n] pamoja na nchi ya
Gileadi,[o] likamkutanikia Yeho-
va katika Mispa.[p] **2** Kwa hiyo

SURA 19

a Amu 19:2
b Law 20:10
c Yer 5:8
Ho 9:9
Ho 10:9
Efe 4:19
d Amu 19:21
e Amu 19:2
Amu 19:25
f Amu 20:5
g Amu 19:18
h Amu 20:6
i Yos 14:1
1Sa 11:7
j Amu 20:7
Met 15:22

SURA 20

k Kum 13:12
Yos 22:12
Amu 21:5
l 1Sa 11:7
2Sa 19:14
m Yos 19:47
Amu 18:29
2Sa 3:10
1Nya 21:2
2Nya 30:5
n 1Sa 3:20
2Sa 24:2
o Yos 22:9
p 1Sa 7:5
1Sa 10:17
2Fa 25:23

Safu ya 2

a Zb 83:18
Isa 44:8
b Amu 20:17
2Sa 24:9
2Fa 3:26
c Amu 20:1
d Amu 19:22
e Amu 19:1
f Amu 19:12
g Amu 19:2
h Amu 19:25
i Amu 19:26
j Amu 19:29
k Law 19:29
Law 20:14
Zb 119:150
Met 10:23
1Pe 4:3
l Amu 19:23
m Amu 19:30
Met 11:14
Met 13:10
Met 20:18
Met 24:6
n Amu 20:1
o Met 21:3
p Amu 1:1
Amu 20:18
1Sa 14:42
Ne 11:1
Met 16:33
Mdo 1:26

wakuu wa watu wote na maka-
bila yote ya Israeli wakasimama
katika kutaniko la watu wa Mu-
ngu wa kweli,[a] wanaume mia
nne elfu wanaoenda kwa mi-
guu, wenye kutumia upanga.[b]

3 Na wana wa Benyamini
wakasikia kwamba wana wa
Israeli wamepanda kwenda Mi-
spa.[c]

Ndipo wana wa Israeli wa-
kasema: "Semeni. Jambo hili
baya limetokea namna gani?"[d]
4 Kwa hiyo yule mtu, Mlawi,[e]
mume wa mwanamke aliyeua-
wa, akajibu na kusema: "Nilie-
nda Gibea,[f] la Benyamini, mimi
na suria[g] wangu, ili tulale usi-
ku kucha. **5** Na wenye ma-
shamba wote wa Gibea wakasi-
mama kunipinga, wakaizungu-
ka nyumba juu yangu wakati
wa usiku. Walikusudia kuniua
mimi, lakini wakamlala kingu-
vu[h] suria wangu, naye mwisho-
we akafa.[i] **6** Basi nikamshika
suria wangu, nikamkatakata vi-
pande na kumpeleka katika
kila shamba la urithi wa Israe-
li,[j] kwa sababu walikuwa wame-
tenda mwenendo mpotovu[k] na
upumbavu wenye kufedhehe-
sha katika Israeli.[l] **7** Tazame-
ni! Enyi nyote wana wa Israe-
li, semeni neno na shauri lenu[m]
hapa."

8 Basi watu wote wakasima-
ma kama mtu mmoja,[n] waki-
sema: "Hatutaenda hata mmo-
ja wetu katika hema lake, wala
hatutageuka hata mmoja wetu
kwenda nyumbani kwake.[o]
9 Na sasa hili ndilo jambo tu-
takalotendea Gibea. Na tupa-
nde kwa kura[p] kwenda kupiga-
na na jiji hilo. **10** Nasi tuchu-
kue watu kumi kati ya mia moja
wa makabila yote ya Israeli, na
mia moja kati ya elfu moja, na
elfu moja kati ya elfu kumi, ili

kuwachukulia watu vyakula, ili
wachukue hatua kwa kwenda
kupigana na Gibea la Benya-
mini, kwa sababu ya huu upu-
mbavu wote wenye kufedhehe-
sha[a] waliotenda katika Israeli."
11 Kwa hiyo wanaume wote wa
Israeli wakakusanyika juu ya
jiji hilo kama mtu mmoja, wasa-
idiane.

12 Ndipo makabila yote ya
Israeli wakatuma watu waende
kwa watu wote wa kabila la Be-
nyamini,[b] wakisema: "Ni jambo
gani hili baya ambalo limefa-
nywa kati yenu?[c] **13** Na sasa
watoeni wale wanaume,[d] wale
watu wasiofaa kitu,[e] ambao
wamo katika Gibea,[f] ili tuwaue,[g]
nasi tuondolee mbali lililo baya
katika Israeli."[h] Na wana wa Be-
nyamini hawakutaka kuisikili-
za sauti ya ndugu zao, wana wa
Israeli.[i]

14 Ndipo wana wa Be-
nyamini wakakusanyika pa-
moja kutoka katika majiji kwe-
nda Gibea ili watoke kupigana
na wana wa Israeli. **15** Basi
wana wa Benyamini wakakusa-
nywa siku hiyo kutoka katika
majiji, watu 26,000 wenye ku-
tumia upanga,[j] mbali na wakaa-
ji wa Gibea, ambao watu 700
waliochaguliwa walikusanywa.
16 Kati ya watu hao wote kuli-
kuwa na watu 700 waliochagu-
liwa, wenye kutumia mkono wa
kushoto.[k] Kila mmoja wa hao
alikuwa mtupa-mawe[l] kwa ko-
mbeo na angeweza kupiga sha-
baha unywele, bila kukosea.

17 Na watu wa Israeli wali-
kusanywa mbali na Benyamini,
wanaume mia nne elfu wenye
kutumia upanga.[m] Kila mmo-
ja wao alikuwa mwanamume
wa vita. **18** Kisha wakasima-
ma, wakapanda kwenda Bethe-
li, wakaulize kutoka kwa Mu-
ngu.[a] Ndipo wana wa Israeli wa-
kasema: "Ni nani kati yetu ata-
kayeongoza pigano juu ya wana
wa Benyamini?"[b] Yehova akase-
ma: "Yuda ataongoza."[c]

19 Kisha wana wa Israeli wa-
kasimama asubuhi na kupiga
kambi juu ya Gibea.

20 Basi watu wa Israeli wa-
katoka kwenda kupigana na
Benyamini; nao wana wa Israeli
wakajipanga kivita juu yao ka-
tika Gibea. **21** Kwa hiyo wana
wa Benyamini wakatoka kati-
ka Gibea,[d] wakawaangusha chi-
ni na kuwaangamiza watu
22,000 katika Israeli siku hiyo.[e]
22 Hata hivyo, watu, wanau-
me wa Israeli, wakaonyesha
uhodari, kisha wakajipanga ki-
vita tena mahali pale walipo-
kuwa wamejipanga kivita siku
ya kwanza. **23** Basi wana wa
Israeli wakapanda na kulia[f]
mbele za Yehova mpaka jioni
nao wakauliza kutoka kwa Ye-
hova, wakisema: "Je, niende ni-
karibie tena kupigana na wana
wa Benyamini ndugu yangu?"[g]
Yehova akasema: "Panda upiga-
ne naye."

24 Basi wana wa Israeli wa-
kawakaribia wana wa Benyami-
ni siku ya pili.[h] **25** Benyami-
ni nao wakatoka katika Gibea
ili kukutana nao siku ya pili,
kisha wakawaangusha chini na
kuwaangamiza[i] watu kumi na
nane elfu tena kati ya wana wa
Israeli, wote hao wakiwa we-
nye kutumia upanga.[j] **26** Basi
wana wote wa Israeli,[k] watu
wote, wakapanda na kuja Be-
theli, wakalia[l] na kukaa hapo
mbele za Yehova nao wakafu-
nga[m] siku hiyo mpaka jioni, wa-
katoa matoleo ya kuteketezwa[n]
na matoleo ya ushirika[o] mbele
za Yehova. **27** Kisha wana wa
Israeli wakauliza kutoka kwa

SURA 20

a Mwa 34:7
Amu 19:23
Amu 19:25
2Sa 13:12
b Yos 18:11
c Kum 13:14
Yos 22:16
Efe 5:11
d 2Sa 20:21
e Amu 19:22
Amu 19:25
f Amu 19:12
g Law 20:10
h Kum 13:5
Kum 17:7
Kum 22:22
1Ko 5:6
1Ko 5:13
i 1Sa 2:25
Met 29:1
Ho 9:9
Ho 10:9
Ro 9:18
j Hes 26:41
k Amu 3:15
l Mwa 49:27
1Sa 17:40
1Sa 17:49
1Nya 12:2
2Nya 26:14
m Amu 20:2

Safu ya 2

a Kut 28:30
Hes 27:21
Amu 20:27
Met 3:6
b Amu 1:1
c Mwa 49:8
Hes 10:14
Amu 1:2
1Nya 5:2
d Amu 19:12
Ho 10:9
e Mwa 49:27
Zb 33:16
Yer 12:1
f Amu 20:26
Met 3:5
Met 16:3
g Amu 20:28
h Amu 20:19
i Amu 20:21
j Amu 20:17
k Amu 20:2
l Amu 20:23
m 2Nya 20:3
Ezr 8:21
Yoe 1:14
n Law 1:3
o Law 3:1
Law 19:5
Amu 21:4
1Sa 10:8

Yehova,[a] kwa kuwa hapo ndipo lilipokuwa lile sanduku la agano[b] la Mungu wa kweli siku hizo. **28** Basi Finehasi[c] mwana wa Eleazari, mwana wa Haruni, alikuwa amesimama mbele ya sanduku hilo siku hizo,[d] akisema: "Je, niende tena kupigana na wana wa Benyamini ndugu yangu, au je, nisiende?"[e] Na Yehova akasema: "Panda, kwa kuwa kesho nitamtia mkononi mwako."[f] **29** Ndipo Israeli wakaweka watu wa kuvizia[g] Gibea pande zote.

30 Na wana wa Israeli wakapanda kwenda juu ya wana wa Benyamini siku ya tatu, wakajipanga kivita kupigana na Gibea kama vile ilivyokuwa nyakati zile nyingine.[h] **31** Wana wa Benyamini walipotoka kwenda kukutana na wale watu, wakavutwa mbali na jiji.[i] Ndipo, kama vile ilivyokuwa zile nyakati nyingine, wakaanza kuwapiga baadhi ya watu, karibu watu 30 katika Israeli,[j] waliokuwa na majeraha ya kufisha katika njia kuu, moja ya njia hizo inapanda kwenda Betheli[k] na ile nyingine inaenda Gibea,[l] shambani. **32** Basi wana wa Benyamini wakaanza kusema: "Wanashindwa mbele yetu kama ilivyokuwa pale mwanzoni."[m] Lakini wana wa Israeli wakasema: "Na tukimbie,[n] nasi hakika tutawavuta mbali kutoka katika jiji, waingie katika njia kuu." **33** Na watu wote wa Israeli wakasimama kutoka mahali pao, kisha wakajipanga kivita katika Baal-tamari, huku wale wa Israeli waliokuwa wakivizia[o] wakifanya mashambulizi kutoka mahali pao katika ujirani wa Gibea.[p] **34** Basi wanaume elfu kumi waliochaguliwa kutoka katika Israeli yote wakaja mbele ya Gibea, na mapigano yalikuwa makali; na Wabenyamini hawakujua kwamba msiba[a] ulikuwa unawakaribia.

35 Naye Yehova akashinda Benyamini[b] mbele ya Israeli, hivi kwamba wana wa Israeli siku hiyo wakaangamiza katika Benyamini watu 25,100, wote hao wenye kutumia upanga.[c]

36 Hata hivyo, wana wa Benyamini walifikiri kwamba watu wa Israeli wangeshindwa[d] walipoendelea kurudi nyuma mbele ya Benyamini kwa sababu walitegemea kile kikundi cha kuvizia ambacho walikuwa wameweka juu ya Gibea. **37** Na wale waliokuwa wakivizia, walitenda haraka, wakatimua mbio kuelekea Gibea.[e] Ndipo wenye kuvizia[f] wakasambaa na kulipiga jiji lote kwa makali ya upanga.[g]

38 Basi watu wa Israeli walikuwa wamefanya mpango na wale wenye kuvizia kwamba wafanye moshi upande juu kama ishara kutoka katika jiji hilo.[h]

Ikabodi,[a] akisema: "Utukufu
umeondoka katika Israeli kwe-
nda uhamishoni,"[b] hayo alise-
ma kuhusu sanduku la Mu-
ngu wa kweli lililotekwa na
kuhusu baba-mkwe wake na
mume wake.[c] **22** Basi akase-
ma: "Utukufu umeondoka kati-
ka Israeli kwenda uhamishoni,[d]
kwa sababu sanduku la Mungu
wa kweli limetekwa."[e]

5 Basi Wafilisti wakalichu-
kua lile sanduku[f] la Mu-
ngu wa kweli, wakalibeba ku-
toka Ebenezeri mpaka Ashdo-
di.[g] **2** Na Wafilisti wakali-
chukua sanduku la Mungu
wa kweli, wakaliingiza ndani
ya nyumba ya Dagoni na ku-
lisimamisha kando ya Dago-
ni.[h] **3** Kisha Waashdodi waka-
amka mapema kesho yake, na
tazama, Dagoni alikuwa ame-
anguka kifudifudi mbele ya
sanduku la Yehova.[i] Basi wa-
kamchukua Dagoni na kumru-
disha mahali pake.[j] **4** Walipo-
amka asubuhi na mapema siku
iliyofuata, tazama, Dagoni ali-
kuwa ameanguka kifudifudi
mbele ya sanduku la Yehova,
huku kichwa cha Dagoni na
mikono yake miwili ikiwa ime-
katwa, mpaka kwenye kizingi-
ti.[k] Ni sehemu yenye umbo la
samaki peke yake ndiyo iliyo-
achwa ikiwa juu yake. **5** Ndi-
yo sababu makuhani wa Da-
goni na wote wanaoingia kati-
ka nyumba ya Dagoni hawa-
kikanyagi kizingiti cha Dagoni
katika Ashdodi mpaka leo hii.

6 Na mkono wa Yehova[l] uka-
wa mzito juu ya Waashdodi,
naye akaanza kusababisha wasi-
wasi mkubwa na kuwapiga kwa
bawasiri,[m] yaani, Ashdodi na
maeneo yake. **7** Na watu wa
Ashdodi wakaona kwamba iko
hivyo, ndipo wakasema: "Msia-
che sanduku la Mungu wa Isra-
eli likae pamoja nasi, kwa saba-
bu mkono wake umekuwa mzito
juu yetu na juu ya Dagoni mu-
ngu wetu."[a] **8** Basi wakawa-
tuma watu wawakusanye kwao
wakuu wote wa muungano wa
Wafilisti, wakasema: "Tutali-
fanyia nini sanduku la Mungu
wa Israeli?" Mwishowe wakase-
ma: "Acheni sanduku la Mungu
wa Israeli lizunguke kwenda Ga-
thi."[b] Basi wakalibeba sanduku
la Mungu wa Israeli kwa kuzu-
nguka mpaka huko.

9 Na ikawa kwamba walipo-
kuwa wamezunguka kulileta
huko, mkono wa Yehova[c] uka-
ja kuwa juu ya jiji hilo na kule-
ta mvurugo mkubwa sana, naye
akaanza kuwapiga watu wa jiji,
kuanzia mdogo hata mkubwa,
na bawasiri[d] zikaanza kulipuka
juu yao. **10** Basi wakalipele-
ka sanduku la Mungu wa kweli
mpaka Ekroni.[e] Na ikawa kwa-
mba mara tu sanduku la Mungu
wa kweli lilipofika Ekroni, Wa-
ekroni wakaanza kulia, wakise-
ma: "Wamelileta sanduku la
Mungu wa Israeli kwangu kwa
kuzunguka ili waniue mimi na
watu wangu!"[f] **11** Kwa hiyo
wakatuma watu wakawakusa-
nya wakuu wote wa muungano
wa Wafilisti na kusema: "Ondo-
eni sanduku la Mungu wa Isra-
eli, lirudi mahali pake, ili lisi-
niue mimi na watu wangu."
Kwa maana mvurugo wa ku-
leta kifo ulikuwa umetokea ka-
tika jiji zima;[g] mkono wa Mu-
ngu wa kweli ulikuwa umeku-
wa mzito sana huko,[h] **12** na
watu ambao hawakufa waliku-
wa wamepigwa na bawasiri.[i] Na
kilio[j] cha jiji hilo cha kuomba

SURA 4
a 1Sa 14:3
b 1Sa 4:5
1Sa 4:11
Zb 78:61
c 1Sa 2:32
1Sa 2:34
d Kum 28:15
e 1Sa 4:11
2Nya 8:11
Yer 7:12

SURA 5
f 1Sa 4:11
1Sa 4:17
Zb 78:61
g Yos 11:22
1Sa 6:17
Mdo 8:40
h Amu 16:23
1Nya 10:10
Zb 115:4
i Kut 12:12
1Nya 16:26
Zb 95:3
Zb 96:5
Zb 97:7
Isa 19:1
Sef 2:11
j Isa 46:7
k Isa 2:18
Yer 10:11
l Kut 9:3
1Sa 5:9
1Sa 5:11
1Sa 7:13
m Kum 28:27
1Sa 6:5

Safu ya 2
a 1Ko 8:5
b 1Sa 17:4
c Kum 2:15
1Sa 7:13
d 1Sa 5:6
e Yos 15:45
Amu 1:18
2Fa 1:2
Amo 1:8
f 1Sa 5:7
g Ebr 10:31
h 1Sa 5:9
i Kum 28:27
j Zb 115:6
Da 5:23
Hab 2:19

msaada kikaendelea kupanda
mpaka mbinguni.

6 Na sanduku[a] la Yehova lili-
kuwa katika eneo la Wafili-
sti kwa miezi saba. **2** Nao Wa-
filisti wakawaita makuhani na
waaguzi,[b] wakisema: "Tulifa-
nyie nini sanduku la Yehova?
Tuambieni tunapaswa kuliru-
disha mahali pake likiwa pamo-
ja na nini." **3** Nao wakasema:
"Ikiwa mnalirudisha sanduku la
Mungu wa Israeli, msilirudi-
she bila toleo, kwa maana kwa
vyovyote mnapaswa kumrudi-
shia toleo la hatia.[c] Ndipo mta-
kapoponywa, nanyi mtajua kwa
nini mkono wake haukuondoka
juu yenu." **4** Ndipo wakasema:
"Tunapaswa kumrudishia toleo
gani la hatia?" Nao wakasema:
"Kulingana na hesabu ya wakuu
wa muungano[d] wa Wafilisti, ba-
wasiri tano za dhahabu na panya
watano wa dhahabu, kwa maa-
na kila mmoja wenu na wakuu
wenu wa muungano wana tau-
ni ileile. **5** Nanyi mfanye sana-
mu za bawasiri zenu na sana-
mu za panya[e] wenu wanaoiha-
ribu nchi, na kumpa utukufu[f]
Mungu wa Israeli. Labda atapu-
nguza uzito wa mkono wake
kutoka juu yenu na juu ya mu-
ngu wenu na juu ya nchi yenu.[g]
6 Pia, kwa nini mfanye mioyo
yenu kuwa migumu kama vile
Misri na Farao walivyofanya mi-
oyo yao kuwa migumu?[h] Je, hai-
kuwa ni mara tu Yeye alipowa-
tendea vikali[i] ndipo walipowaa-
chilia waende zao, nao wakaen-
da zao?[j] **7** Na sasa chukueni
na kutengeneza gari jipya la ku-
kokotwa,[k] na ng'ombe wawili
wanaonyonyesha, ambao hawa-
jawekwa nira[l] yoyote juu yao,
nanyi mwafunganishe ng'ombe
hao na lile gari, nanyi mwa-
rudishe ndama wao nyumbani

SURA 6

a 1Sa 4:11
1Sa 5:1
Zb 78:61

b Kut 7:11
Law 19:31
Kum 18:12
Isa 2:6

c 1Sa 6:4
1Sa 6:17

d Yos 13:3
Amu 3:3
1Sa 6:16

e Law 11:29
1Sa 6:18
Isa 66:17

f 1Nya 16:28
Zb 18:44
Isa 42:12

g Kut 9:3
1Sa 5:6
1Sa 5:11

h Kut 7:13
Kut 8:15
Kut 14:17
Ro 9:18

i Kut 9:14
Kut 9:16
Ro 9:17

j Kut 6:1
Kut 11:1
Kut 12:33
Zb 105:38

k 2Sa 6:3
1Nya 13:7

l Hes 19:2

Safu ya 2

a 1Sa 6:4

b 1Sa 6:3

c Yos 15:10
Yos 21:16
2Fa 14:11
1Nya 6:59
2Nya 28:18

d Mhu 9:11

e 2Sa 6:3
1Nya 13:7

f 1Sa 6:9

g Yos 13:3
Amu 3:3
1Sa 6:4

h Ru 2:2
Ru 2:23

ili wasiwafuate. **8** Na mlichu-
kue sanduku la Yehova mli-
weke juu ya lile gari, na vile
vyombo vya dhahabu[a] amba-
vyo mtamrudishia kama toleo
la hatia[b] mviweke ndani ya sa-
nduku kando yake. Nanyi mna-
paswa kuliacha liende, nalo
linapaswa kwenda. **9** Nanyi
mnapaswa kutazama: likipa-
nda barabara inayoelekea kwe-
nye eneo lake, kuelekea Beth-
shemeshi,[c] basi yeye ndiye ame-
tutendea huu uovu mkubwa;
lakini kama sivyo, tutajua kwa-
mba haukuwa mkono wake uli-
otugusa; bali ni msiba[d] tu
uliotuangukia."

10 Na watu wakafanya hi-
vyo. Kwa hiyo wakachukua
ng'ombe wawili wanaonyonye-
sha, wakawafunganisha na lile
gari, na ndama wao wakawafu-
ngia nyumbani. **11** Kisha wa-
kaliweka sanduku la Yehova juu
ya lile gari,[e] na pia lile sandu-
ku na wale panya wa dhaha-
bu na sanamu za bawasiri zao.
12 Na wale ng'ombe wakaa-
nza kwenda mbele moja kwa
moja kwenye barabara inayo-
elekea Beth-shemeshi.[f] Wakae-
nda katika ile njia kuu moja,
huku wakilia wakiwa wanae-
nda, nao hawakugeuka kando
upande wa kuume wala wa ku-
shoto. Wakati huohuo wale wa-
kuu wa muungano[g] wa Wafili-
sti walikuwa wakitembea nyu-
ma yao hadi kwenye mpaka wa
Beth-shemeshi. **13** Na watu
wa Beth-shemeshi walikuwa
wakivuna mavuno ya ngano[h]
katika nchi tambarare ya chi-
ni. Walipoinua macho yao na
kuona lile Sanduku, wakaa-
nza kushangilia kwa kuliona.
14 Nalo gari likaja katika sha-
mba la Yoshua Mbeth-shemeshi,
likasimama pale, ambapo pali-

kuwa na jiwe kubwa. Nao wakaanza kupasua mbao za lile gari, na kuwatoa wale ng'ombe[a] kuwa toleo la kuteketezwa kwa Yehova.[b]

15 Nao Walawi[c] wakalishusha sanduku la Yehova na lile sanduku lililokuwa pamoja nalo, ambamo ndani yake mlikuwa vile vyombo vya dhahabu, wakaliweka juu ya lile jiwe kubwa. Na watu wa Beth-shemeshi[d] wakatoa matoleo ya kuteketezwa, wakaendelea kumtolea Yehova dhabihu siku hiyo.

16 Na wale wakuu watano wa muungano[e] wa Wafilisti wakaona hayo, nao wakarudi Ekroni siku hiyo. **17** Basi hizi ndizo bawasiri za dhahabu ambazo Wafilisti walirudisha kuwa toleo la hatia kwa Yehova:[f] kwa ajili ya Ashdodi[g] moja, kwa ajili ya Gaza[h] moja, kwa ajili ya Ashkeloni[i] moja, kwa ajili ya Gathi[j] moja, kwa ajili ya Ekroni[k] moja. **18** Na wale panya wa dhahabu walilingana na hesabu ya majiji yote ya Wafilisti ya wale wakuu watano wa muungano, kuanzia jiji lenye ngome mpaka kijiji cha nchi iliyo wazi.

Na lile jiwe kubwa ambalo juu yake waliweka sanduku la Yehova ni ushahidi mpaka leo hii katika shamba la Yoshua, Mbeth-shemeshi. **19** Naye akawapiga watu wa Beth-shemeshi,[l] kwa maana walikuwa wamelitazama sanduku la Yehova. Basi kati ya watu akapiga na kuua watu 70—watu 50,000—kisha watu wakaanza kuomboleza kwa sababu Yehova alikuwa amewapiga watu hao kwa mauaji makubwa.[m] **20** Na zaidi, watu wa Beth-shemeshi wakasema: "Ni nani atakayeweza kusimama mbele za Yehova, huyu Mungu mtakatifu,[a] naye ataondoka kwetu aende kwa nani?"[b] **21** Mwishowe wakatuma wajumbe kwa wakaaji wa Kiriath-yearimu,[c] wakisema: "Wafilisti wamelirudisha sanduku la Yehova. Shukeni. Mlichukue na kulipandisha kwenu."[d]

7 Basi watu wa Kiriath-yearimu[e] wakaja, nao wakalipandisha sanduku la Yehova na kuliingiza katika nyumba ya Abinadabu[f] juu ya kilima, nao wakamtakasa Eleazari mwana wake ili alinde sanduku la Yehova.

2 Na ikawa kwamba tangu siku ambayo hilo Sanduku lilikaa katika Kiriath-yearimu, siku zikaendelea kuongezeka, nazo zikawa jumla ya miaka 20, na nyumba yote ya Israeli wakamwombolezea Yehova.[g] **3** Na Samweli akaiambia nyumba yote ya Israeli: "Ikiwa mnarudi kwa Yehova[h] kwa mioyo yenu yote, ondoeni miungu ya kigeni iliyo katikati yenu[i] na pia zile sanamu za Ashtorethi,[j] nanyi mwelekeze mioyo yenu kwa Yehova bila kuyumba-yumba, mkamtumikie yeye peke yake,[k] naye atawakomboa kutoka mkono wa Wafilisti."[l] **4** Kwa hiyo wana wa Israeli wakaondoa Mabaali[m] na sanamu za Ashtorethi,[n] wakaanza kumtumikia Yehova peke yake.

5 Kisha Samweli akasema: "Kusanyeni Israeli[o] wote katika Mispa,[p] ili nisali[q] kwa Yehova kwa ajili yenu." **6** Basi wakakusanyika pamoja kule Mispa, nao wakachota maji na kuyamwaga mbele za Yehova na kufunga siku hiyo.[r] Nao

SURA 6

a Mwa 15:9; 1Sa 6:7; 1Sa 16:2
b Kut 20:24; Amu 21:4
c Hes 3:31
d Yos 21:16
e 1Sa 6:12
f 1Sa 6:4
g 1Sa 5:1; 2Nya 26:6; Yer 25:20; Zek 9:6; Mdo 8:40
h Amu 16:1; Amu 16:21; Amo 1:7; Mdo 8:26
i Amu 1:18; Zek 9:5
j 1Sa 5:8; 1Sa 17:4; 2Sa 21:22
k Yos 13:3; 1Sa 5:10; 2Fa 1:2; Amo 1:8
l Yos 15:10; Yos 21:16; 1Sa 6:9
m Hes 4:6; Hes 4:15; Hes 4:20; 1Nya 13:10

Safu ya 2

a Law 11:45; 1Sa 2:2
b Hes 17:12; 2Sa 6:9; 1Nya 13:12; Zb 76:7
c Yos 18:14; Amu 18:12; 1Nya 13:5
d 1Nya 13:6; 1Nya 16:1; 2Nya 1:4

SURA 7

e 2Sa 6:2; 1Nya 13:5
f 2Sa 6:4; 1Nya 13:7
g Amu 2:4; Ne 9:28; 2Ko 7:10
h Kum 30:2; 1Sa 12:24; 1Fa 8:48; Isa 55:7; Yoe 2:12
i Yos 24:14; Yos 24:23; Amu 3:7; Amu 10:6
j Amu 2:13
k Kum 6:13; Kum 10:20; Kum 13:4; Lu 4:8
l Kum 28:1
m Amu 10:16
n 1Fa 11:33
o Yoe 2:16
p Yos 18:26; Amu 20:1; Amu 21:1; 1Sa 10:17; 1Fa 15:22; 2Fa 25:23; Yer 40:6
q 1Sa 12:23; Met 15:8; Yak 5:16

r 2Nya 20:3; Ne 9:1; Yoe 2:12.

wakaanza kusema huko: "Tumemtendea dhambi Yehova."[a]
Naye Samweli akawahukumu[b]
wana wa Israeli katika Mispa.
7 Na Wafilisti wakaja kusikia kwamba wana wa Israeli
wamekusanyika Mispa, na wale
wakuu wa muungano[c] wa Wafilisti wakapanda juu ya Israeli. Wana wa Israeli waliposikia habari hizo, wakaanza kuogopa kwa sababu ya Wafilisti.[d]
8 Kwa hiyo wana wa Israeli wakamwambia Samweli: "Usikae
kimya kwa ajili yetu ukose kumwomba Yehova Mungu wetu
msaada,[e] atukomboe kutoka
mkono wa Wafilisti." **9** Ndipo Samweli akachukua mwana-kondoo anayenyonya, akamtoa kwa Yehova kuwa toleo
la kuteketezwa,[f] toleo zima;
na Samweli akaanza kumwomba Yehova msaada kwa ajili
ya Israeli,[g] naye Yehova akamjibu.[h] **10** Na ikawa kwamba Samweli alipokuwa akitoa lile
toleo la kuteketezwa, Wafilisti wakasonga karibu ili kupigana na Israeli. Na huko Yehova
akafanya kuwe na mngurumo
wa sauti kubwa[i] siku hiyo juu
ya Wafilisti, ili awavuruge;[j] nao
wakashindwa mbele ya Israeli.[k]
11 Ndipo watu wa Israeli wakafanya mashambulizi kutoka
Mispa na kuwafuatilia Wafilisti,
wakaendelea kuwapiga mpaka
upande wa kusini wa Beth-kari.
12 Kisha Samweli akachukua
jiwe[l] na kulisimamisha kati
ya Mispa na Yeshana, akaliita
jina Ebenezeri. Basi akasema:
"Yehova ametusaidia mpaka
sasa."[m] **13** Kwa hiyo Wafilisti
wakatiishwa, wala hawakuingia
tena katika eneo la Israeli;[n] na
mkono wa Yehova ukaendelea
kuwa juu ya Wafilisti siku zote
za Samweli.[o] **14** Na yale majiji
ambayo Wafilisti walikuwa wameyachukua kutoka kwa Israeli yakaendelea kurudi kwa Israeli kutoka Ekroni mpaka Gathi,
na Israeli wakayakomboa maeneo ya majiji hayo kutoka mkono wa Wafilisti.
Na kukawa na amani kati ya
Israeli na Waamori.[a]
15 Na Samweli akaendelea
kuhukumu Israeli siku zote
za maisha yake.[b] **16** Naye
akasafiri mwaka baada ya mwaka na kufanya mzunguko wa
Betheli[c] na Gilgali[d] na Mispa[e]
na kuhukumu Israeli[f] katika sehemu hizo zote. **17** Lakini alikuwa akirudi Rama,[g] kwa sababu nyumba yake ilikuwa huko,
naye akahukumu Israeli huko.
Naye akamjengea Yehova madhabahu huko.[h]

8 Na ikawa kwamba mara Samweli alipokuwa amezeeka, akawaweka[i] wanawe kuwa
waamuzi wa Israeli. **2** Basi
jina la mwana wake mzaliwa wa
kwanza lilikuwa Yoeli,[j] na jina
la wa pili Abiya;[k] walikuwa wakihukumu katika Beer-sheba.
3 Na wanawe hawakutembea
katika njia zake,[l] bali walikuwa na mwelekeo wa kufuata faida isiyo ya haki[m] na wakawa wakikubali rushwa[n] na kupotosha
hukumu.[o]
4 Baada ya muda wanaume
wazee wote wa Israeli[p] wakakusanyika pamoja na kumjia
Samweli katika Rama **5** na
kumwambia: "Tazama! Wewe
mwenyewe umezeeka, lakini
wana wako hawakutembea katika njia zako. Basi sasa tuchagulie mfalme[q] wa kutuhukumu sisi kama mataifa mengine
yote." **6** Lakini jambo hilo lilikuwa baya machoni pa Sa-

SURA 7
a Law 26:40 Amu 10:10 1Fa 8:47 Zb 106:6
b Amu 2:18
c Yos 13:3 1Sa 6:4
d Zb 56:3 Met 29:25 Mt 10:28
e 1Sa 12:19 Zb 78:34 Zb 86:7 Isa 37:4
f Law 1:10 Amu 6:26 1Fa 18:38
g Zb 99:6
h Zb 28:6 Zb 50:15 1Yo 5:14
i 1Sa 2:10 2Sa 22:14
j Yos 10:10 Amu 4:15
k Kum 20:4 Kum 28:7
l Mwa 31:45 Mwa 35:14 Yos 4:9 Yos 24:26
m Zb 44:3 Mdo 26:22
n 1Sa 9:16 1Sa 13:5
o 1Sa 14:23 1Sa 17:51

Safu ya 2
a Mwa 15:18 Mwa 15:21 Amu 11:23
b Amu 2:16 1Sa 3:20 1Sa 12:11 1Sa 25:1 Mdo 13:20
c Yos 16:1
d Yos 15:7 1Sa 11:15
e 1Sa 7:5
f 1Sa 3:20 1Sa 12:11
g 1Sa 1:1 1Sa 8:4 1Sa 19:18
h Kut 20:25

SURA 8
i 1Ti 5:22
j 1Nya 6:28
k 1Nya 6:28
l Mhu 2:19
m Kut 18:21 1Ti 3:3 1Pe 5:2
n Kut 23:8 Kum 16:19 Zb 15:5 Zb 26:10 Met 29:4 Isa 1:23 Isa 33:15 Mik 3:11
o Kum 24:17 Ayu 34:12 Met 31:5 Yer 22:17
p Kut 18:25 Amu 21:16 1Sa 4:3 2Sa 5:3 1Fa 20:7

q Kum 17:14; 1Sa 12:13; Ho 13:10; Mdo 13:21.

mweli kwa vile walikuwa wamesema: "Tupe mfalme atuhukumu," na Samweli akaanza kusali kwa Yehova.[a] **7** Ndipo Yehova akamwambia Samweli:[b] "Sikiliza sauti ya watu kuhusu mambo yote wanayokuambia;[c] kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi nisiwe mfalme[d] juu yao. **8** Kulingana na matendo yao yote ambayo wametenda tangu siku nilipowatoa kutoka Misri[e] mpaka leo hii kwa kuwa walizidi kuniacha[f] na kuitumikia miungu mingine,[g] hivyo ndivyo wanavyokutendea wewe pia. **9** Basi sasa sikiliza sauti yao. Ila tu, unapaswa kuwaonya kwa uzito, nawe ni lazima uwaambie kile ambacho ni haki ya mfalme atakayetawala juu yao."[h]

10 Basi Samweli akawaambia wale watu waliokuwa wakimwomba awape mfalme maneno yote ya Yehova. **11** Naye akasema: "Hili ndilo litakalokuwa fungu ambalo ni haki[i] ya mfalme atakayetawala juu yenu: Atawachukua wana wenu[j] na kuwaweka kama wanawe katika magari[k] yake na kati ya wapanda-farasi[l] wake, na baadhi yao watakimbia mbele ya magari[m] yake; **12** na kujichagulia wakuu wawe juu ya watu 1,000[n] na wakuu wawe juu ya watu 50,[o] na baadhi yao wamlimie[p] na kuvuna mavuno[q] yake na kutengeneza silaha zake za vita[r] na vyombo vya magari yake.[s] **13** Naye atachukua binti zenu wawe wachanganyaji wa marhamu na wapishi na waokaji.[t] **14** Na mashamba yenu na mizabibu[u] yenu na mizeituni[v] yenu, iliyo bora zaidi, atachukua na kuwapa watumishi wake. **15** Na kutoka nafaka ya mashamba yenu na mazao ya mashamba yenu ya mizabibu atachukua sehemu ya kumi,[a] naye atawapa maofisa[b] wake wa makao ya mfalme na watumishi wake. **16** Atachukua watumishi wenu wanaume na wajakazi wenu na mifugo yenu iliyo bora zaidi, na punda wenu, naye atawatumia kwa kazi yake.[c] **17** Atachukua sehemu ya kumi kutoka makundi[d] yenu, nanyi mtakuwa watumishi wake. **18** Nanyi mtalia siku hiyo kwa sababu ya mfalme wenu,[e] ambaye mlijichagulia wenyewe, lakini Yehova hatawajibu siku hiyo."[f]

19 Hata hivyo, watu wakakataa kuisikiliza sauti ya Samweli[g] na kusema: "Hapana, bali mfalme atakuwa juu yetu. **20** Na sisi pia, lazima tuwe kama mataifa mengine yote,[h] na mfalme wetu lazima atuhukumu na kwenda mbele yetu na kupigana vita vyetu." **21** Naye Samweli akasikiliza maneno yote ya watu hao; kisha akayasema masikioni mwa Yehova.[i] **22** Naye Yehova akamwambia Samweli: "Sikiliza sauti yao, nawe ufanye mfalme awatawale."[j] Basi Samweli akawaambia watu wa Israeli: "Kila mmoja aende kwenye jiji lake."

9 Basi palikuwa na mtu wa Benyamini, na jina lake lilikuwa Kishi,[k] mwana wa Abieli, mwana wa Zerori, mwana wa Bekorathi, mwana wa Afia, Mbenyamini,[l] mtu mwenye nguvu ya mali.[m] **2** Naye alikuwa na mwana ambaye jina lake lilikuwa Sauli,[n] kijana na mwenye sura nzuri, wala hakuwako mwanamume yeyote wa wana wa Israeli aliyekuwa na sura nzuri kuliko yeye; kutoka kwenye mabega yake kwenda juu alikuwa mrefu kuliko watu wote.[o]

SURA 8
a Zb 143:10
Mt 6:10
b 1Sa 15:10
Zb 99:6
c Zb 81:12
d Amu 8:23
1Sa 10:19
1Sa 12:12
Zb 74:12
Isa 33:22
e Kut 14:30
f Kum 9:24
Yer 22:21
g Kum 32:16
Amu 2:19
Zb 78:58
h Kum 17:15
i 1Sa 10:25
j 1Sa 14:52
1Fa 12:4
k 1Fa 9:22
1Fa 10:26
l 1Fa 4:26
m 2Sa 8:4
2Sa 15:1
1Fa 1:5
n 2Sa 18:1
1Nya 27:1
o 2Fa 1:14
p 1Nya 27:26
q 1Fa 4:7
r 1Nya 12:37
s 1Fa 4:26
t 1Fa 4:22
u 1Fa 21:7
v 1Nya 27:28

Safu ya 2
a 1Fa 12:10
b Mwa 37:36
1Nya 28:1
c 1Fa 5:16
d 1Fa 4:23
e 1Fa 12:4
f Ayu 27:9
Zb 18:41
Met 1:26
Mik 3:4
g Zb 81:11
Yer 7:13
Eze 33:31
h Law 20:24
Hes 23:9
Kum 7:6
1Sa 8:5
Zb 106:35
i Zb 99:6
j 1Sa 8:7
Ho 13:11

SURA 9
k 1Sa 14:51
1Nya 8:33
1Nya 9:39
Mdo 13:21
l Amu 21:17
m 1Sa 25:2
2Sa 19:32
Ayu 1:3
n 1Sa 11:15
1Sa 13:13
1Sa 15:26
1Sa 16:23
1Sa 28:7
1Sa 31:4
2Sa 1:23
Mdo 13:21
o 1Sa 10:23

3 Na punda-jike[a] za Kishi
baba ya Sauli wakapotea. Basi
Kishi akamwambia Sauli mwa-
na wake: "Tafadhali, chukua
pamoja nawe mmoja wa watu-
mishi, uondoke, uende kuwata-
futa hao punda-jike." **4** Naye
akaenda, akipita katika eneo
lenye milima la Efraimu,[b] akae-
ndelea, akapita katika nchi ya
Shalisha,[c] wala hawakuwapa-
ta. Nao wakaendelea, wakapi-
ta katika nchi ya Shaalimu,
lakini hawakuwa huko. Naye
akaendelea, akapita katika nchi
ya Wabenyamini, wala hawa-
kuwapata.
5 Nao wakaingia katika nchi
ya Sufu; na Sauli akamwa-
mbia mtumishi wake aliyekuwa
pamoja naye: "Haya njoo, turu-
di, ili baba yangu asije akaa-
cha kufikiri juu ya punda-jike na
kuanza kuhangaika juu yetu."[d]
6 Lakini yeye akamwambia:
"Tafadhali, tazama! Kuna mtu
wa Mungu[e] katika jiji hili, na
mtu huyo anaheshimiwa. Kila
jambo analosema hutimia bila
kukosa.[f] Na twende huko sasa.
Labda anaweza kutuambia njia
yetu tunayopaswa kuiendea."
7 Ndipo Sauli akamwambia
mtumishi wake: "Na tukienda,
tutampelekea mtu huyo nini?[g]
kwa maana mkate umekwisha
katika vyombo vyetu, wala ha-
kuna zawadi[h] yoyote ya kumpe-
lekea huyo mtu wa Mungu wa
kweli. Tuna nini pamoja nasi?"
8 Basi mtumishi akamjibu Sau-
li tena na kusema: "Tazama!
Kuna sehemu ya nne ya she-
keli[i] ya fedha mkononi mwa-
ngu, nami nitampa huyo mtu
wa Mungu wa kweli, naye ata-
tuambia njia yetu." **9** (Nyakati
za kale katika Israeli, mtu aliku-
wa akisema hivi akienda kumta-
futa Mungu: "Haya njooni, na
twende kwa mwonaji."[a] Kwa ma-
ana nabii wa leo alikuwa aki-
itwa mwonaji nyakati za kale.)
10 Ndipo Sauli akamwambia
mtumishi wake: "Neno lako ni
jema.[b] Haya njoo, twende."
Nao wakaenda zao kwenye jiji
lile alilokuwamo mtu wa Mungu
wa kweli.
11 Walipokuwa wakipanda
kwenda jijini, wakakuta wasi-
chana wakitoka kwenda kute-
ka maji.[c] Basi wakawauliza: "Je,
mwonaji[d] yuko mahali hapa?"
12 Nao wakawajibu na kusema:
"Ndiyo. Tazama! Yuko mbe-
le yenu. Fanyeni haraka sasa,
kwa sababu amekuja jijini leo,
kwa maana leo kuna dhabihu[e]
kwa ajili ya watu katika maha-
li pa juu.[f] **13** Mara mtakapo-
ingia jijini, mtamkuta moja
kwa moja kabla hajapanda kwe-
nda mahali pa juu ili ale cha-
kula; kwa kuwa watu hawawe-
zi kula mpaka aje, kwa maana
yeye ndiye anayeibariki dhabi-
hu.[g] Baadaye wale walioalikwa
hula. Basi sasa pandeni—sasa
hivi mtampata." **14** Nao wa-
kapanda kwenda jijini. Walipo-
kuwa wakiingia katikati ya jiji,
tazama, Samweli alikuwa ana-
toka nje kuja kuwapokea ili ku-
panda kwenda mahali pa juu.
15 Naye Yehova alikuwa
amefunua sikio[h] la Samweli ile
siku iliyotangulia kuja kwa Sa-
uli, akisema: **16** "Karibu wa-
kati kama huu kesho nitatuma
mtu kwako kutoka katika nchi
ya Benyamini,[i] nawe umtie ma-
futa[j] awe kiongozi juu ya watu
wangu Israeli; naye atawaokoa
watu wangu kutoka mkononi
mwa Wafilisti,[k] kwa sababu ni-
meona mateso ya watu wangu,
kwa maana kilio chao kimeni-
fikia."[l] **17** Na Samweli aka-
mwona Sauli, naye Yehova aka-

SURA 9
a Amu 5:10
Amu 10:4
b Yos 17:10
Yos 17:16
c 2Fa 4:42
d 1Sa 9:20
1Sa 10:2
e Kum 33:1
1Sa 2:27
1Fa 13:1
2Fa 6:6
f 1Sa 3:19
Isa 44:26
Zek 1:6
Ebr 1:1
g 1Fa 14:3
2Fa 4:42
Ga 6:6
h 2Fa 5:15
2Fa 8:8
Met 17:8
Met 18:16
i Mwa 24:22

Safu ya 2
a 1Sa 9:19
2Sa 15:27
1Nya 9:22
1Nya 29:29
b Met 13:10
Met 15:22
c Mwa 24:20
Kut 2:16
d 1Sa 9:19
2Sa 15:27
e Mwa 31:54
1Sa 7:9
1Sa 16:5
f 1Fa 3:2
1Nya 16:39
2Nya 1:3
g Mk 6:41
Lu 9:16
h 1Sa 20:2
2Sa 7:27
Ayu 33:16
Zb 25:14
Zb 99:6
Amo 3:7
i Yos 18:11
j 1Sa 10:1
1Sa 15:1
2Fa 9:3
k Mwa 49:27
l Kut 2:25
Zb 106:44
Zb 107:19

mjibu: “Huyu ndiye mtu niliyekuambia, ‘Huyu ndiye atakayewazuia watu wangu wasipite mipaka.’”[a]

18 Ndipo Sauli akamkaribia Samweli katikati ya lango na kusema: “Tafadhali niambie, Nyumba ya mwonaji iko wapi?” **19** Naye Samweli akamjibu Sauli na kusema: “Mimi ndiye mwonaji. Panda mbele yangu, uende mahali pa juu, nanyi mtakula pamoja nami leo,[b] nami nitawaacha mwende zenu asubuhi, nami nitakuambia mambo yote yaliyo moyoni mwako.[c] **20** Na wale punda-jike uliowapoteza siku tatu zilizopita,[d] usitie moyo[e] wako juu yao, kwa maana wamepatikana. Na je, vitu vyote vyenye kutamanika vya Israeli ni vya nani?[f] Je, si vyako na vya nyumba yote ya baba yako?” **21** Ndipo Sauli akajibu na kusema: “Je, mimi si Mbenyamini wa kutoka katika kabila dogo zaidi[g] kati ya makabila ya Israeli,[h] na je, familia yangu si dhaifu zaidi kati ya familia zote za kabila la Benyamini?[i] Basi kwa nini umeniambia jambo kama hili?”[j]

22 Ndipo Samweli akamchukua Sauli na mtumishi wake, akawaleta katika jumba la kulia chakula, akawapa viti mbele[k] ya wale walioalikwa; nao walikuwa karibu watu 30. **23** Baadaye Samweli akamwambia mpishi: “Leta lile fungu nililokupa, ambalo juu yake nilikuambia hivi, ‘Liweke kando yako.’” **24** Kwa hiyo yule mpishi akainua ule mguu na ile nyama iliyokuwa juu yake, akauweka mbele ya Sauli. Naye akasema tena: “Kilichowekwa akiba ndicho hiki. Kiweke mbele yako. Ule, kwa maana wamekuwekea hicho akiba mpaka wakati uliowekwa ili ule pamoja na wale walioalikwa.” Basi Sauli akala pamoja na Samweli siku hiyo. **25** Kisha wakashuka kutoka mahali pa juu,[a] wakaenda jijini, naye akaendelea kusema na Sauli darini.[b] **26** Nao wakaamka mapema na ikawa, mara kulipopambazuka, Samweli akamwita Sauli juu darini, akisema: “Simama, nikuache uende zako.” Basi Sauli akasimama na wote wawili, yeye na Samweli, wakatoka nje. **27** Walipokuwa wakishuka ukingoni mwa jiji, Samweli akamwambia Sauli: “Mwambie mtumishi[c] apite mbele yetu”—basi akapita—“nawe simama tuli sasa ili nikuambie neno la Mungu.”

10 Ndipo Samweli akachukua chupa[d] ya mafuta na kuyamimina juu ya kichwa chake, akambusu[e] na kusema: “Je, si kwa sababu Yehova amekutia mafuta uwe kiongozi[f] juu ya urithi wake?[g] **2** Utakapoondoka kwangu leo hakika utakuta watu wawili karibu na kaburi la Raheli[h] katika eneo la Benyamini katika Selsa, nao watakuambia, ‘Wale punda-jike ambao ulienda kutafuta wamepatikana, lakini sasa baba yako ameacha habari za wale punda-jike[i] naye anawahangaikia ninyi, akisema: “Nitafanya nini kwa ajili ya mwanangu?”’[j] **3** Nawe utapita kutoka hapo na kusonga mbele zaidi, uje mpaka kwenye ule mti mkubwa wa Tabori, na hapo wanaume watatu watakutana nawe, wakipanda kwenda kwa Mungu wa kweli katika Betheli,[k] mmoja akiwa amebeba wana-mbuzi[l] watatu na mwingine akiwa amebeba mikate mitatu ya mviringo[m] na mwingine

SURA 9
a 1Sa 10:24
1Sa 15:17
Mdo 13:21
b 1Sa 9:13
1Sa 9:24
c 1Nya 28:9
Ebr 4:13
d 1Sa 9:3
e 1Sa 4:20
f 1Sa 8:5
1Sa 8:19
1Sa 12:13
g Amu 20:46
Amu 20:47
Amu 21:6
Zb 68:27
h Amu 21:3
i Amu 6:15
Met 3:34
Met 11:2
Met 18:12
Met 22:4
Lu 14:11
Yak 4:6
1Pe 5:5
j 1Sa 2:8
k Lu 14:10

Safu ya 2
a 1Sa 9:13
1Sa 9:19
1Fa 3:2
1Fa 3:3
b Ne 8:16
Mdo 10:9
c 1Sa 9:3
1Sa 9:10
1Sa 20:38

SURA 10
d 1Sa 16:13
2Fa 9:3
e Mwa 31:55
Mwa 48:10
Mwa 50:1
2Sa 19:39
f Mwa 49:27
1Sa 8:9
1Sa 9:16
Mdo 13:21
g Kut 19:5
Kum 32:9
h Mwa 35:19
i 1Sa 9:3
1Sa 10:16
j 1Sa 9:5
k Mwa 28:19
Mwa 28:22
1Sa 7:16
l Amu 6:19
Amu 15:1
m Yer 37:21

akiwa amebeba mtungi mkubwa wa divai.[a] **4** Na watauliza habari za hali yako[b] na kukupa mikate miwili, nawe uikubali kutoka mkononi mwao. **5** Ni baada ya hapo kwamba utakuja kwenye kilima cha Mungu wa kweli,[c] palipo na kambi ya kijeshi[d] ya Wafilisti. Na itakuwa kwamba wakati utakapokuja hapo kwenye jiji, utakutana na kikundi cha manabii[e] wakishuka kutoka mahali pa juu,[f] na mbele yao kukiwa na kinanda[g] na tari[h] na filimbi[i] na kinubi,[j] huku wakisema kama manabii. **6** Na roho[k] ya Yehova hakika itaanza kutenda kazi juu yako, kisha utasema kama nabii[l] pamoja nao, nawe utabadilishwa uwe mtu mwingine. **7** Na itakuwa kwamba ishara[m] hizo zitakapokuja juu yako, jifanyie lile ambalo mkono wako unaweza,[n] kwa sababu Mungu wa kweli yupo pamoja nawe.[o] **8** Nawe ushuke mbele yangu kwenda Gilgali;[p] na tazama! ninashuka kuja kwako ili nitoe dhabihu za kuteketezwa, ili nitoe dhabihu za ushirika.[q] Uendelee kungojea siku saba[r] mpaka nitakapokujia, nami hakika nitakujulisha yale unayopaswa kufanya."

9 Na ikawa kwamba mara tu alipogeuza bega lake aende zake kutoka kwa Samweli, Mungu akaanza kuubadili moyo wake uwe mwingine;[s] na ishara[t] hizo zote zikatimia siku hiyo. **10** Basi wakatoka hapo wakaenda kwenye kilima, na tazama, kulikuwa na kikundi cha manabii kikija kumpokea; ndipo mara moja roho ya Mungu ikaanza kutenda kazi juu yake,[u] naye akaanza kusema kama nabii[v] katikati yao. **11** Na ikawa kwamba wakati watu wote waliokuwa wakimjua hapo zamani walipomwona, tazama! alikuwa akitoa unabii pamoja na manabii. Basi watu wakaambiana: "Ni nini hili lililompata mwana wa Kishi? Je, Sauli pia yumo kati ya manabii?"[a] **12** Ndipo mtu mmoja kutoka hapo akajibu na kusema: "Lakini baba yao ni nani?" Ndiyo sababu kumekuwa na neno la kimethali:[b] "Je, Sauli pia yumo kati ya manabii?"

13 Mwishowe akamaliza kusema kama nabii, akaja mahali pa juu. **14** Baadaye ndugu ya baba ya Sauli akamwambia yeye na mtumishi wake: "Mlienda wapi?" Naye akasema: "Kuwatafuta wale punda-jike,[c] nasi tukaendelea kwenda ili tuone, lakini hawakuwapo. Basi tukaenda kwa Samweli." **15** Kisha ndugu ya baba ya Sauli akasema: "Tafadhali niambieni, Samweli aliwaambia nini?" **16** Sauli naye akamwambia ndugu ya baba yake: "Alituambia kwa uhakika kwamba wale punda-jike walikuwa wamepatikana." Lakini yeye hakumwambia lile jambo la ufalme, ambalo Samweli alikuwa amesema.[d]

17 Na Samweli akawaita watu pamoja waje mbele za Yehova kule Mispa[e] **18** na kuwaambia wana wa Israeli: "Yehova, Mungu wa Israeli amesema hivi,[f] 'Mimi ndiye niliyewatoa Israeli kutoka Misri nami nikawakomboa ninyi kutoka mkono wa Misri[g] na kutoka mkono wa falme zote zilizokuwa zikiwakandamiza ninyi.[h] **19** Lakini ninyi—leo mmemkataa Mungu[i] wenu ambaye alikuwa mwokozi wenu kutoka katika maovu yenu yote na taa-

SURA 10

a Law 23:13
Hes 15:5
b Amu 18:15
c Mwa 5:22
d 1Sa 13:3
e 1Sa 19:20
2Fa 2:3
2Fa 4:38
2Fa 6:1
f 1Sa 9:12
g 1Nya 13:8
h 1Sa 18:6
i 1Fa 1:40
Isa 5:12
j 2Sa 6:5
1Fa 10:12
1Nya 16:5
k Hes 11:25
Mdo 28:25
2Pe 1:21
l 1Sa 10:10
1Sa 19:23
1Fa 18:29
1Fa 22:10
m Kut 4:8
1Sa 10:9
Yer 44:29
n Amu 9:33
o Kum 20:1
Amu 6:12
p 1Sa 7:16
1Sa 11:14
q 1Sa 13:9
r 1Sa 13:8
s 1Sa 10:6
1Fa 3:12
Zb 51:10
t 1Sa 10:7
Isa 38:7
u Amu 14:6
1Sa 11:6
1Sa 16:13
Zek 4:6
2Ko 3:5
v 1Sa 10:6
1Sa 19:23

Safu ya 2

a 1Sa 19:24
Mt 13:54
Mdo 6:15
b Ayu 27:1
Zb 78:2
c 1Sa 9:3
d Zb 141:3
Met 10:19
Met 13:3
Met 21:23
Met 27:2
Yer 9:23
e 1Sa 7:5
f Kum 18:20
g Kut 13:14
Kut 14:30
Kum 4:34
Amu 6:8
Ne 9:9
h Ne 9:27
Zb 107:19
i 1Sa 8:7
1Sa 12:12

bu zenu, nanyi mkasema: "Hapana, bali uweke mfalme juu yetu." Basi sasa simameni mbele za Yehova kulingana na makabila[a] yenu na kulingana na maelfu yenu.'"

20 Basi Samweli akafanya makabila yote ya Israeli yakaribie,[b] nalo kabila la Benyamini likachaguliwa.[c] **21** Kisha akafanya kabila la Benyamini likaribie kulingana na familia zao, ndipo familia ya Wamatri ikachaguliwa.[d] Mwishowe Sauli mwana wa Kishi akachaguliwa.[e] Nao wakamtafuta, lakini hakupatikana. **22** Kwa hiyo wakamuuliza[f] tena Yehova: "Je, mtu huyo amekwisha kuja hapa?" Ndipo Yehova akasema: "Tazama, amejificha[g] kati ya mizigo." **23** Basi wakakimbia na kumchukua kutoka hapo. Aliposimama katikati ya watu, alikuwa mrefu kuliko watu wengine wote kuanzia mabega yake na kwenda juu.[h] **24** Ndipo Samweli akawaambia watu wote: "Je, mmemwona yule ambaye Yehova amemchagua,[i] kwamba hakuna yeyote kama yeye kati ya watu wote?" Nao watu wote wakaanza kupiga kelele na kusema: "Mfalme na aishi!"[j]

25 Kwa hiyo Samweli akasema na watu kuhusu fungu ambalo ni haki ya ufalme[k] na kuandika hayo katika kitabu na kukiweka mbele za Yehova. Kisha Samweli akawaacha watu wote waende zao, kila mmoja nyumbani kwake. **26** Bali Sauli akaenda nyumbani kwake kule Gibea,[l] na wanaume mashujaa ambao Mungu alikuwa amegusa mioyo yao wakaenda pamoja naye.[m] **27** Lakini watu wasiofaa kitu[n] wakasema: "Huyu atatuokoa vipi?"[o] Basi wakamdharau,[p] wala hawakumletea zawadi yoyote.[a] Lakini yeye akaendelea kuwa kama mtu asiyeweza kusema.[b]

11 Na Nahashi Mwamoni[c] akapanda na kupiga kambi juu ya Yabeshi[d] katika Gileadi. Kwa hiyo watu wote wa Yabeshi wakamwambia Nahashi: "Fanya agano pamoja nasi ili tukutumikie."[e] **2** Ndipo Nahashi Mwamoni akawaambia: "Nitafanya agano pamoja nanyi kwa sharti hili, kwa sharti la kung'oa[f] kila jicho lenu la kuume, nami ni lazima niweke jambo hilo kuwa shutuma juu ya Israeli wote."[g] **3** Nao wanaume wazee wa Yabeshi wakamwambia: "Tupatie muda wa siku saba, nasi tutatuma wajumbe katika eneo lote la Israeli, na, ikiwa hatutapata mwokozi,[h] ndipo tutalazimika kuja kwako." **4** Baadaye hao wajumbe wakaja Gibea[i] la Sauli na kusema maneno hayo masikioni mwa watu, na watu wote wakaanza kupaaza sauti zao na kulia.[j]

5 Lakini tazama, Sauli akija nyuma ya mifugo yake kutoka shambani, naye Sauli akasema: "Watu wana nini, kwamba walie?" Wakaanza kumsimulia maneno ya wale watu wa Yabeshi. **6** Na roho[k] ya Mungu ikaanza kutenda kazi juu ya Sauli alipoyasikia maneno hayo, hasira yake ikawaka sana.[l] **7** Kwa hiyo akachukua ng'ombe-dume wawili, akawakata vipande-vipande, akavipeleka katika eneo lote la Israeli[m] kwa mkono wa wajumbe, akisema: "Yeyote kati yetu ambaye hatatoka akiwa mfuasi wa Sauli na Samweli, ng'ombe zake watafanywa hivi!"[n] Na hofu[o] ya Yehova[p] ikaanza kuwashika watu hivi kwamba wakatoka kama

SURA 10

a 2Nya 30:6
b Yos 7:14
Mdo 1:24
c Yos 7:16
1Sa 9:21
d Yos 7:17
e Yos 7:18
Mdo 13:21
f Amu 1:1
Amu 20:18
Amu 20:28
1Sa 23:2
g 1Sa 9:21
Met 11:2
Lu 9:48
h 1Sa 9:2
i Kum 17:15
1Sa 9:17
j 1Fa 1:25
1Fa 1:39
2Fa 11:12
Mt 21:9
k 1Sa 8:11
l Yos 18:28
Amu 20:14
1Sa 11:4
1Sa 13:2
2Sa 21:6
m Ezr 1:5
n 2Sa 20:1
2Nya 13:7
Nah 1:15
o 1Sa 11:12
Mdo 7:51
p Mhu 10:20

Safu ya 2

a 1Fa 10:10
2Nya 17:5
Met 18:16
Mt 2:11
b Met 17:27
Ga 5:23
Yak 1:19

SURA 11

c Kum 2:19
d Amu 21:8
1Sa 31:11
e Kum 23:3
f Amu 16:21
2Fa 25:7
g Met 18:3
h Amu 3:9
i 1Sa 10:26
1Sa 14:2
j Amu 2:4
Amu 21:2
1Sa 30:4
k Amu 3:10
Amu 6:34
Amu 11:29
Amu 14:6
1Sa 10:10
1Sa 16:13
l Kut 11:8
Kut 32:19
Ro 12:9
m Amu 19:29
n Amu 21:5
o 1Nya 14:17
p Mwa 35:5
2Nya 14:14
2Nya 17:10

mtu mmoja.[a] **8** Ndipo akahesabu[b] watu hao katika Bezeki,
na wana wa Israeli wakawa jumla ya 300,000, na watu wa
Yuda 30,000. **9** Basi wakawaambia wale wajumbe ambao wa-
likuwa wamekuja: "Hivi ndivyo mtakavyowaambia watu wa Ya-
beshi katika Gileadi, 'Kesho mtapata wokovu wakati wa jua
kali.'"[c] Basi wale wajumbe wakaja na kuwaambia watu wa Ya-
beshi, nao wakaanza kushangilia. **10** Kwa hiyo watu wa Ya-
beshi wakasema: "Kesho tutawajia ninyi, nanyi mtutendee
kulingana na yote yaliyo mema machoni penu."[d]

11 Na ikawa kesho yake kwamba Sauli[e] akaweka watu
katika vikosi vitatu;[f] nao wakaingia katikati ya kambi wakati
wa kesha la kuamkia asubuhi[g] na kuwapiga Waamoni[h] mpa-
ka wakati siku ilipokuwa na jua kali. Na baadhi yao walipo-
onekana kuwa wamebaki, ndipo wakatawanywa, wala hawa-
kubaki watu wawili wakiwa pamoja kati yao.[i] **12** Na watu
wakaanza kumwambia Samweli: "Ni nani wanaosema, 'Je, Sa-
uli atakuwa mfalme juu yetu?'[j] Watoeni watu hao, ili tuwaue."[k]
13 Hata hivyo, Sauli akasema: "Mtu yeyote asiuawe leo,[l] kwa
maana leo Yehova ametimiza wokovu katika Israeli."[m]

14 Baadaye Samweli akawaambia watu: "Njooni, twe-
nde Gilgali,[n] ili tuufanye upya ufalme huko."[o] **15** Basi watu
wote wakaenda Gilgali, kisha wakamfanya Sauli kuwa mfa-
lme mbele za Yehova katika Gilgali. Ndipo wakatoa huko dha-
bihu za ushirika mbele za Yehova,[p] na Sauli na watu wote wa
Israeli wakaendelea kushangilia huko kwa hali ya juu sana.[q]

SURA 11

a Amu 20:8
b 1Sa 13:15
c Zb 18:17
d 1Sa 11:3
e 1Sa 9:16
f Amu 7:16
Amu 9:43
Met 24:6
g Kut 14:24
h 1Sa 11:1
i Kum 28:7
Zb 21:8
Zb 21:12
j 1Sa 10:27
Met 24:21
k Met 25:5
Lu 19:27
l 2Sa 19:22
Met 20:28
Ro 12:19
m 1Sa 19:5
1Nya 11:14
Zb 44:7
Isa 59:16
n 1Sa 7:16
o 1Sa 10:17
1Sa 10:24
p Law 7:11
1Sa 10:8
q 1Fa 1:40
2Fa 11:14
1Nya 12:40
Ufu 19:6

Safu ya 2

SURA 12

a 1Sa 8:5
1Sa 8:21
b 1Sa 10:24
1Sa 11:14
c Hes 27:17
1Sa 8:20
d 1Sa 8:1
e Zb 71:18
Met 16:31
Met 20:29
Isa 46:4
f 1Sa 8:3
Eze 18:20
g 1Sa 3:19
Zb 99:6
h 1Sa 9:16
1Sa 10:1
1Sa 24:6
2Sa 1:14
Mdo 4:27
Mdo 10:38
i Hes 16:15
j Kum 16:19
k Kut 22:4
Law 6:4
Lu 19:8
l Zb 37:6
Da 6:4
1Ti 3:2
m 1Sa 26:11
n Zb 17:3
Zb 37:37
Yoh 18:38
Mdo 20:33
1Th 2:5
o Kut 6:26
Ne 9:14
Zb 77:20
Zb 105:26
Ho 12:13
Mik 6:4
p Amu 5:11
q Mwa 46:6
Hes 20:15
Mdo 7:15
r Kut 2:23
Kut 3:9
s Kut 3:10

12 Mwishowe Samweli akawaambia Israeli wote:
"Tazama, nimesikiliza sauti
yenu kuhusu mambo yote
ambayo mmeniambia,[a] kwa-
mba nifanye mfalme atawa-
le juu yenu.[b] **2** Na sasa taza-
meni, mfalme anatembea mbele
yenu![c] Lakini mimi nimezeeka[d]
nami nina mvi,[e] na tazameni,
wanangu wako pamoja nanyi,[f]
nami nimetembea mbele yenu
tangu ujana wangu mpaka leo
hii.[g] **3** Mimi hapa. Leteni jibu
kinyume changu mbele za Ye-
hova na mbele ya mtiwa-mafu-
ta[h] wake: Nimechukua ng'ombe
wa nani au nimechukua punda
wa nani[i] au nimempunja nani
au nimemponda nani au nime-
pokea kutoka kwa mkono wa
nani pesa za hongo ili nizitu-
mie kufunga macho yangu?[j]
Nami nitawarudishia ninyi."[k]
4 Nao wakasema: "Wewe huku-
tupunja, wala kutuponda, wala
kupokea chochote kutoka mko-
noni mwa mtu hata mmoja."[l]
5 Basi akawaambia: "Yehova ni
shahidi dhidi yenu, na mtiwa-
mafuta[m] wake ni shahidi leo
kwamba hamkupata chochote
mkononi mwangu."[n] Nao waka-
sema: "Yeye ni shahidi."

6 Na Samweli akaendelea
kuwaambia watu hao: "Yehova
ni shahidi, aliyewatumia Musa
na Haruni, na ambaye aliwale-
ta mababu zenu kutoka nchi ya
Misri.[o] **7** Basi sasa simame-
ni, nami nitawahukumu ninyi
mbele za Yehova na kuwasimu-
lia matendo yote ya uadilifu[p] ya
Yehova ambayo amewafanyia
ninyi na mababu zenu.

8 "Mara Yakobo alipokuwa
ameingia Misri[q] nao mababu
zenu wakaanza kumwomba Ye-
hova msaada,[r] Yehova aliwatu-
ma Musa[s] na Haruni, ili wa-

waongoze mababu zenu watoke Misri na kuwakalisha
mahali hapa.[a] **9** Nao wakamsahau Yehova, Mungu wao,[b]
naye akawauza[c] mkononi mwa
Sisera[d] mkuu wa jeshi la Hasori na mkononi mwa Wafilisti[e]
na mkononi mwa mfalme wa
Moabu,[f] nao wakaendelea kupiga vita juu yao. **10** Nao wa-
kaanza kumwomba Yehova
msaada,[g] wakisema, 'Tumetenda dhambi,[h] kwa maana tume-
mwacha Yehova ili tutumikie
Mabaali[i] na sanamu za Ashtorethi;[j] basi sasa utukomboe[k] kutoka mkono wa adui zetu, ili
tukutumikie.' **11** Ndipo Yeho-
va akamtuma Yerubaali[l] na
Bedani na Yeftha[m] na Samweli,[n] akawakomboa kutoka mkono wa adui zenu pande zote,
ili mkae kwa amani.[o] **12** Mli-
poona kwamba Nahashi[p] mfalme wa wana wa Amoni amekuja kupigana nanyi, mkaniambia tena na tena, 'Hapana,
bali ni mfalme ndiye atakayetawala juu yetu!'[q] ingawa wakati
huo wote Yehova Mungu wenu
alikuwa mfalme wenu.[r] **13** Na
sasa tazameni, mfalme mliye-
mchagua, ambaye mliomba;[s]
na tazameni, Yehova ameweka mfalme juu yenu.[t] **14** Mki-
mwogopa[u] Yehova na kumtumi-
kia[v] na kuitii sauti yake[w] kwe-
likweli, nanyi msipoliasi[x] agizo
la Yehova, ninyi pamoja na mfalme atakayetawala juu yenu
mtakuwa wafuasi wa Yehova,
Mungu wenu. **15** Lakini msi-
poisikiliza sauti ya Yehova,[y] na
ikiwa kwelikweli mtaliasi agizo la Yehova,[z] hakika mkono wa
Yehova utakuwa kinyume che-
nu na baba zenu.[a] **16** Sasa,
pia, simameni mwone jambo hili
kubwa ambalo Yehova anafanya mbele ya macho yenu.

SURA 12

a Yos 1:2
Yos 11:23
Zb 44:3
b Kum 32:18
Amu 2:12
Zb 106:39
c Kum 32:30
Amu 2:14
d Amu 4:2
e Amu 10:7
Amu 13:1
f Amu 3:12
g Amu 2:18
Amu 3:9
Amu 6:7
h Amu 10:10
i Amu 3:7
j Amu 2:13
k Amu 10:15
l Amu 6:32
m Amu 11:1
n Ebr 11:32
o Law 26:6
Zb 4:8
p 1Sa 11:1
q 1Sa 8:5
1Sa 8:19
r Kum 33:5
Amu 8:23
1Sa 8:7
Zb 74:12
Isa 33:22
s 1Sa 8:5
t 1Sa 9:16
1Sa 10:24
Ho 13:11
u Kum 10:12
Kum 17:19
v Kum 6:13
Yos 24:14
w Kum 13:4
Kum 28:2
x Hes 14:9
Yos 22:29
y Law 26:14
Kum 28:15
z Yos 24:20
a Law 26:17
Hes 33:56
Kum 28:45

Safu ya 2

a Met 26:1
b 1Sa 7:9
Yak 5:16
c Yak 5:17
d 1Sa 8:7
Ho 13:11
e 1Fa 18:37
f 1Fa 18:1
g 1Sa 7:5
1Sa 12:23
Met 15:8
Mdo 8:24
Yak 5:16
h Kut 20:20
i Kum 11:16
Kum 31:29
Yos 23:6
1Sa 12:15
j Kum 6:5
Mt 22:37
k Kum 32:21
Yer 2:5
Yer 2:11
1Ko 8:4
l Zb 115:5
Yer 10:15
Yer 16:19
Hab 2:18
m 1Fa 6:13
Zb 94:14
Ro 11:1

17 Je, leo si mavuno ya ngano?[a]
Nitamwomba[b] Yehova ili alete
mngurumo na mvua;[c] ndipo
mjue na kuona kwamba uovu
wenu ni mwingi[d] ambao mmefa-
nya machoni pa Yehova kwa kujiombea mfalme."

18 Ndipo Samweli akamwita
Yehova,[e] naye Yehova akaleta
mngurumo na mvua siku hiyo,[f]
hivi kwamba watu wote waka-
waogopa sana Yehova na Samweli. **19** Na watu wote wa-
kaanza kumwambia Samweli:
"Sali[g] kwa Yehova Mungu wako
kwa ajili ya watumishi wako,
kwa maana hatutaki kufa; kwa
sababu tumeongeza uovu juu
ya dhambi zetu zote kwa kujiombea mfalme."

20 Basi Samweli akawaam-
bia watu: "Msiogope.[h] Ninyi
—mmefanya uovu huu wote. Ila
tu msigeuke kando mwache ku-
mtumikia Yehova,[i] nanyi lazima
mmtumikie Yehova kwa moyo
wenu wote.[j] **21** Nanyi msigeu-
ke kando ili kufuata vitu visi-
vyo vya kweli[k] ambavyo ha-
vina faida[l] yoyote na amba-
vyo havikomboi, kwa sababu
hivyo ni vitu visivyo vya kwe-
li. **22** Kwa maana Yehova ha-
tawaacha[m] watu wake kwa aji-
li ya jina lake kuu,[n] kwa saba-
bu Yehova ameamua mwenye-
we kuwafanya ninyi kuwa watu
wake.[o] **23** Nami pia, kwa upa-
nde wangu, ni jambo lisilowa-
ziwa, kwamba nimtendee Yeho-
va dhambi kwa kuacha kusali
kwa ajili yenu;[p] nami nitawa-
fundisha[q] ninyi katika njia ili-
yo njema[r] na iliyo sawa. **24** Ila
tu mwogopeni[s] Yehova, nanyi
mkamtumikie katika kweli kwa

n Yos 7:9; Zb 23:3; Zb 106:8; Yer 14:21; Eze 20:14; o Kut 19:5; Kum 7:7; Kum 14:2; Kum 32:9; Isa 43:21; p Ro 1:9; Kol 1:9; 2Ti 1:3; q Zb 34:11; Met 4:11; r 1Fa 8:36; 2Nya 6:27; s 1Sa 12:14; Zb 111:10; Mhu 12:13.

moyo wenu wote;[a] kwa maana
angalieni jinsi amewafanyia ma-
mbo makuu.[b] **25** Lakini mki-
fanya yaliyo mabaya bila kujali,
ninyi pamoja na mfalme wenu[c]
mtafagiliwa mbali."[d]

13 Sauli alikuwa na umri
wa miaka [?] alipoanza
kutawala,[e] naye akatawala mia-
ka miwili juu ya Israeli. **2** Na
Sauli akajichagulia watu elfu
tatu katika Israeli; na elfu mbili
walikuwa pamoja na Sauli huko
Mikmashi[f] na katika eneo le-
nye milima la Betheli, na elfu
moja wakawa pamoja na Yona-
thani[g] huko Gibea[h] la Benyami-
ni, naye akawaacha watu wale
wengine waende zao, kila mmo-
ja kwenye hema lake. **3** Ndi-
po Yonathani akaipiga kambi ya
kijeshi[i] ya Wafilisti[j] iliyokuwa
katika Geba;[k] nao Wafilisti wa-
kasikia habari hizo. Naye Sauli
akapiga baragumu[l] nchini kote,
akisema: "Waebrania na wasi-
kie!" **4** Na Israeli wote waka-
sikia habari: "Sauli ameipiga ka-
mbi ya kijeshi ya Wafilisti, na
sasa Israeli wamekuwa haru-
fu mbaya[m] kwa Wafilisti." Basi
watu wakakusanywa pamoja,
wamfuate Sauli huko Gilgali.[n]
5 Nao Wafilisti, kwa upande
wao, wakakusanyika pamoja ili
kupigana na Israeli, magari ya
vita 30,000[o] na wapanda-farasi
6,000 na watu wengi kama che-
mbe za mchanga kando ya ba-
hari;[p] nao wakaondoka, waka-
panda na kupiga kambi katika
Mikmashi upande wa mashari-
ki wa Beth-aveni.[q] **6** Na watu
wa Israeli wakaona kwamba
wako katika shida kali,[r] kwa
sababu watu walikuwa wame-
banwa sana; na watu wakajifi-
cha katika mapango[s] na mashi-
mo na miamba na ngome na
mashimo ya maji. **7** Hata Wa-
ebrania wakavuka Yordani[a]
kwenda katika nchi ya Gadi[b]
na Gileadi. Lakini Sauli aliku-
wa bado katika Gilgali, na watu
wote wakamfuata wakitetemeka.[c] **8** Naye akaendelea ku-
ngojea siku saba mpaka waka-
ti uliowekwa ambao Samweli
alikuwa amesema;[d] na Samweli
hakuja Gilgali, na watu wakawa
wanatawanyika kutoka kwa-
ke. **9** Mwishowe Sauli akase-
ma: "Leteni karibu nami dhabi-
hu ya kuteketezwa na dhabihu
za ushirika." Basi akaitoa dha-
bihu ya kuteketezwa.[e]
10 Na ikawa kwamba mara
alipokuwa amemaliza kuitoa
dhabihu ya kuteketezwa, ta-
zama, Samweli alikuwa anai-
ngia. Basi Sauli akatoka kwe-
nda kumpokea na kumbari-
ki.[f] **11** Ndipo Samweli akase-
ma: "Umefanya nini?"[g] Naye
Sauli akasema: "Niliona kwa-
mba watu wametawanyika ku-
toka kwangu,[h] nawe hukuja
katika siku zilizowekwa,[i] na
Wafilisti walikuwa wakikusa-
nyika pamoja huko Mikmashi,[j]
12 basi nikasema moyoni mwa-
ngu,[k] 'Sasa Wafilisti watashuka
juu yangu katika Gilgali, nami
sijautuliza uso wa Yehova.' Kwa
hiyo nikajilazimisha,[l] nikaitoa
dhabihu ya kuteketezwa."
13 Ndipo Samweli akamwa-
mbia Sauli: "Umetenda kipu-
mbavu.[m] Hukuishika amri[n] ya
Yehova Mungu wako ambayo
alikuamuru,[o] kwa sababu, kama
ungeishika, Yehova angeufa-
nya ufalme wako juu ya Israeli
kuwa imara mpaka wakati usio
na kipimo. **14** Lakini sasa
ufalme wako hautadumu.[p] Ye-
hova atajitafutia mtu anayeku-

SURA 12

a Kum 10:12
b Kum 10:21
c Kum 28:36
d Yos 24:20

SURA 13

e Mdo 13:21
f 1Sa 14:5
Isa 10:28
g 1Sa 18:1
2Sa 1:4
2Sa 21:7
h Yos 18:28
1Sa 10:26
1Sa 15:34
i 1Sa 10:5
2Sa 23:14
j Yos 13:2
1Sa 9:16
k Yos 18:24
Yos 21:17
Zek 14:10
l Amu 3:27
Amu 6:34
2Sa 2:28
2Sa 20:1
m Mwa 34:30
Kut 5:21
n Yos 5:9
1Sa 7:16
1Sa 11:14
o Kum 20:1
p Mwa 22:17
Yos 11:4
Amu 7:12
q Yos 7:2
Yos 18:12
1Sa 14:23
r Kum 4:30
s Kum 20:3
1Sa 14:11

Safu ya 2

a Law 26:36
b Hes 32:1
Yos 13:24
c 1Sa 10:26
Met 24:10
d 1Sa 10:8
e 1Sa 15:11
1Sa 15:22
1Sa 15:23
Zb 37:7
Met 11:2
Met 13:10
Met 21:24
f Mwa 47:7
Ru 2:4
1Sa 15:13
1Sa 25:14
g Yos 7:19
Ro 14:12
h Kum 20:1
1Sa 13:6
i 1Sa 13:8
j 1Sa 13:5
k Met 3:5
Met 14:12
Met 19:21
l Met 11:2
Met 21:24
Mik 6:8
m Met 13:21
Mhu 7:17
Yer 5:4
n Zb 119:4
Mhu 12:13
1Yo 5:3
o 1Sa 10:8
1Sa 15:11
p Kum 17:20
1Sa 15:28

balika kwa moyo wake;[a] na Yehova atamweka kuwa kiongozi[b]
juu ya watu wake, kwa sababu
wewe hukushika yale aliyokuamuru Yehova."[c]
15 Kisha Samweli akaondoka, akaenda zake kutoka Gilgali mpaka Gibea la Benyamini, naye Sauli akawahesabu watu, wale waliokuwa bado pamoja naye, karibu watu mia sita.[d] **16** Na Sauli na Yonathani mwana wake na watu waliokuwa bado pamoja nao walikuwa wakikaa katika Geba[e] la Benyamini. Nao Wafilisti walikuwa wamepiga kambi katika Mikmashi.[f] **17** Na vikosi vya waporaji vikawa vikifanya mashambulizi kutoka katika kambi ya Wafilisti vikiwa vikosi vitatu.[g] Kikosi kimoja kikawa kikigeukia kwenye barabara inayoenda Ofra,[h] mpaka nchi ya Shuali, **18** na kile kikosi kingine kikawa kikigeukia kwenye barabara ya Bethhoroni,[i] na kile kikosi cha tatu kikawa kikigeukia kwenye barabara iliyo kwenye mpaka ulio upande wa bonde la Seboimu, kuelekea nyikani.
19 Basi hakuonekana fundi wa chuma yeyote katika nchi yote ya Israeli, kwa sababu Wafilisti walikuwa wamesema: "Ili Waebrania wasitengeneze upanga wala mkuki."[j] **20** Na Waisraeli wote wakawa wakishuka kwenda kwa Wafilisti ili wanolewe kila mmoja wao jembe lake au jembetezo lake au shoka lake au mundu wake.[k] **21** Na bei ya kunoa ikawa ni pimu moja kwa majembe na kwa majembetezo na kwa vifaa vyenye meno matatu na kwa mashoka na kwa kuimarisha mchokoo wa ng'ombe.[l] **22** Na ikawa katika siku ya pigano kwamba haukuonekana upanga[a] wala mkuki mkononi mwa mtu yeyote aliyekuwa pamoja na Sauli na Yonathani; lakini kukapatikana mmoja uliokuwa wa Sauli[b] na wa Yonathani mwana wake.
23 Basi kituo cha mbele[c] cha Wafilisti kikawa kikishambulia kuingia katika kipito cha mfereji cha Mikmashi.[d]

14 Na ikawa siku moja kwamba Yonathani[e] mwana wa Sauli alimwambia mtumishi aliyechukua silaha zake: "Njoo tuvuke, twende kwenye kituo cha mbele cha Wafilisti walio pale ng'ambo." Lakini hakumwambia baba yake jambo hilo.[f] **2** Na Sauli alikuwa akikaa mipakani mwa Gibea[g] chini ya mkomamanga ulio katika Migroni; na watu waliokuwa pamoja naye walikuwa karibu wanaume mia sita.[h] **3** (Na Ahiya mwana wa Ahitubu,[i] ndugu ya Ikabodi,[j] mwana wa Finehasi,[k] mwana wa Eli,[l] kuhani wa Yehova katika Shilo,[m] alikuwa ameibeba efodi.)[n] Nao watu hawakujua kwamba Yonathani alikuwa ameenda. **4** Basi kati ya zile njia ambazo Yonathani alitafuta kuvukia kwenda juu ya kituo cha mbele[o] cha Wafilisti, kulikuwa na mwamba ulio na umbo la jino upande huu na mwamba ulio na umbo la jino upande ule mwingine, na jina la ule mmoja lilikuwa ni Bosesi na jina la ule mwingine lilikuwa ni Sene. **5** Hilo jino moja lilikuwa ni nguzo upande wa kaskazini kuelekea Mikmashi,[p] na lile lingine lilikuwa upande wa kusini kuelekea Geba.[q]
6 Basi Yonathani akamwambia yule mtumishi, mchukuasilaha wake: "Haya njoo, na tuvuke, twende kwenye kituo cha mbele cha wanaume hawa

SURA 13
a 1Sa 16:1
2Sa 7:15
Zb 78:70
Zb 89:20
Mdo 13:22
b Mwa 49:10
2Sa 5:2
2Sa 7:8
1Nya 28:4
c 1Sa 10:8
Yer 7:23
Yer 11:7
d 1Sa 13:7
1Sa 14:2
e Yos 18:24
1Sa 13:3
f 1Sa 13:2
Isa 10:28
g 1Sa 11:11
h Yos 18:23
i Yos 10:11
Yos 18:13
1Nya 6:68
2Nya 8:5
j 2Fa 24:14
k Mwa 4:22
Met 27:17
l Amu 3:31

Safu ya 2
a Amu 7:20
1Sa 17:47
1Sa 17:50
Zb 44:3
Zek 4:6
b 1Sa 9:16
c 1Sa 14:4
d 1Sa 13:2
1Sa 14:5
Isa 10:28

SURA 14
e 1Sa 13:22
1Sa 14:49
1Sa 18:1
2Sa 1:4
2Sa 21:7
f Amu 14:6
g 1Sa 10:26
h 1Sa 13:15
i 1Sa 22:9
j 1Sa 4:21
k 1Sa 2:12
1Sa 4:17
l 1Sa 1:9
m Yos 18:1
1Sa 1:3
n Kut 29:5
Hes 27:21
o 1Sa 13:23
p 1Sa 13:2
q 1Sa 13:3

wasiotahiriwa.[a] Labda Yehova atatenda kwa ajili yetu, kwa maana hakuna kizuizi chochote kwa Yehova kuokoa kwamba ni kwa wengi au ni kwa wachache."[b] **7** Ndipo mchukua-silaha wake akamwambia: "Fanya lolote lililo moyoni mwako. Enda popote unapotaka. Tazama, mimi nipo pamoja nawe kulingana na moyo wako."[c] **8** Ndipo Yonathani akasema: "Tazama, tunavuka kwenda kwa watu wale, nasi tujionyeshe kwao. **9** Wakituambia hivi, 'Simameni tuli mpaka tukutane nanyi!' ndipo tutakaposimama mahali tulipo, nasi tusipande kwenda walipo. **10** Lakini wakisema hivi, 'Njooni juu yetu!' ndipo tutakapopanda, kwa sababu hakika Yehova atawatia mkononi mwetu, na hii itakuwa ndiyo ishara kwetu."[d]

11 Basi hao wawili wakajionyesha kwenye kituo cha mbele cha Wafilisti. Nao Wafilisti wakasema: "Tazama, Waebrania wanatoka katika matundu walimojificha."[e] **12** Kwa hiyo watu wa kituo hicho cha mbele wakamjibu Yonathani na mchukua-silaha wake na kusema: "Njooni hapa juu tulipo, na sisi tutawaonyesha jambo fulani!"[f] Mara moja Yonathani akamwambia mchukua-silaha wake: "Nifuate, kwa kuwa hakika Yehova atawatia mkononi mwa Israeli."[g] **13** Naye Yonathani akaendelea kupanda kwa mikono[h] yake na miguu yake, na mchukua-silaha wake akimfuata; nao wakaanza kuanguka mbele ya Yonathani,[i] na mchukua-silaha wake akawa akiwaua nyuma yake.[j] **14** Na yale mauaji ya kwanza ambayo Yonathani na mchukua-silaha wake waliwapiga yakawa watu karibu 20 ndani ya nafasi inayolingana na karibu nusu ya uwanja unaoweza kulimwa na ng'ombe wawili.

15 Ndipo tetemeko[a] likatokea katika kambi iliyo shambani na katikati ya watu wote wa kile kituo cha mbele; na hata lile jeshi la waporaji[b] likatetemeka, na dunia ikaanza kutetemeka,[c] nalo likawa ni tetemeko kutoka kwa Mungu.[d] **16** Na walinzi wa Sauli waliokuwa katika Gibea[e] la Benyamini wakaona hayo, na tazama! machafuko hayo yalienea pande zote.[f]

17 Ndipo Sauli akawaambia watu waliokuwa pamoja naye: "Tafadhali, fanyeni hesabu, mwone ni nani ambaye ametoka kwetu." Walipohesabu, tazama! Yonathani na mchukua-silaha wake hawakuwepo. **18** Basi Sauli akamwambia Ahiya:[g] "Lilete karibu sanduku la Mungu wa kweli!"[h] (Kwa maana siku hiyo sanduku la Mungu wa kweli lilikuwa pamoja na wana wa Israeli.)[i] **19** Na ikawa kwamba Sauli alipokuwa akisema na kuhani,[j] yale machafuko yaliyokuwa katika kambi ya Wafilisti yakazidi kuendelea, yakawa makubwa zaidi na zaidi. Ndipo Sauli akamwambia yule kuhani: "Rudisha mkono wako." **20** Hivyo Sauli na watu wote waliokuwa pamoja naye wakaitwa nje.[k] Wakaenda mpaka kwenye pigano, na tazama, upanga wa kila mmoja ulikuwa umeinuka juu ya mtu na mwenzake;[l] machafuko yalikuwa makubwa sana. **21** Na wale Waebrania waliokuwa wamekuwa mali ya Wafilisti[m] kama hapo zamani na waliokuwa wamepanda pamoja nao kuingia katika kambi iliyozunguka pande

SURA 14

a Mwa 17:10
Amu 14:3
Amu 15:18
1Sa 17:36
2Sa 1:20
1Nya 10:4
Yer 9:26
b Amu 7:2
2Fa 6:16
2Nya 14:11
Zb 115:11
Ebr 11:33
c 2Fa 10:15
Met 17:17
d Mwa 24:14
Amu 7:11
1Sa 10:7
e 1Sa 13:6
1Sa 14:22
f 1Sa 14:10
1Sa 17:44
2Fa 14:8
g 1Sa 14:6
2Sa 5:24
2Fa 6:16
Met 3:5
Met 16:3
h Zb 18:29
Ebr 11:34
21 Na tazama! nitamtuma mtu-
mishi, nikisema, 'Nenda, tafuta
ile mishale.' Nikimwambia mtu-
mishi waziwazi hivi, 'Tazama!
Mishale iko upande huu wako,
ichukue,' ndipo uje, kwa maana
hilo linamaanisha amani kwa-
ko, wala hakuna jambo, kama
Yehova anavyoishi.[d] **22** Laki-
ni nikimwambia hivi huyo mvu-
lana, 'Tazama! Mishale iko mba-
li zaidi kutoka kwako,' basi ne-
nda, kwa kuwa Yehova ame-
kutuma uende zako. **23** Na
kuhusu neno hili ambalo tume-
sema[e] mimi na wewe, tazama,
Yehova na awe kati yangu na
wewe mpaka wakati usio na ki-
pimo."[f]
24 Ndipo Daudi akajificha
shambani.[g] Nao mwezi mpya
ukafika, naye mfalme akaketi
kula mlo.[h] **25** Na mfalme ali-
kuwa ameketi katika kiti cha-
ke kama katika zile nyakati nyi-
ngine, katika kiti kilicho ka-
ndo ya ukuta; na Yonathani ali-
kuwa anamwelekea, na Abneri[i]
alikuwa ameketi kando ya Sau-
li, lakini mahali pa Daudi pali-
kuwa wazi. **26** Na Sauli haku-
sema lolote siku hiyo, kwa ma-
ana alisema moyoni mwake:
"Jambo fulani limetokea, naye
si safi,[j] kwa kuwa hajatakaswa."

SURA 20
a 1Sa 19:2
b Kut 34:23
Kum 6:13
Yos 24:23
c Ayu 31:4
Zb 17:3
Zb 139:1
d Ru 1:17
1Sa 3:17
1Sa 25:22
2Sa 3:9
e 1Sa 16:13
1Sa 17:37
f 1Sa 10:7
1Sa 11:6
1Sa 14:47
2Sa 1:22
g Yoh 15:13
h 2Sa 9:3
2Sa 9:7
i 2Sa 9:1
2Sa 21:7
j 1Sa 18:3
2Sa 21:7

Safu ya 2
a 1Sa 18:1
2Sa 1:26
Met 18:24
b 1Sa 20:5
Ezr 3:5
Isa 1:13
c 1Sa 19:2
1Sa 20:5
d Kum 6:13
Kum 10:20
Amu 8:19
1Sa 14:39
1Sa 19:6
1Sa 20:3
1Sa 25:26
Mt 5:33
e 1Sa 20:14
f Mwa 16:5
1Sa 20:42
g Met 27:12
h 1Sa 20:5
i 1Sa 14:50
1Sa 17:55
j Law 11:24
Law 15:5
Law 15:16
Law 15:18
Hes 19:16

27 Na ikawa kwamba, katika
siku iliyofuata mwezi mpya, ka-
tika siku ya pili, mahali pa Dau-
di paliendelea kuwa wazi. Kwa
hiyo Sauli akamwambia Yona-
thani mwana wake: "Kwa nini
mwana wa Yese[a] hakuja kwenye
mlo jana wala leo?" **28** Basi
Yonathani akamjibu Sauli: "Da-
udi aliniomba kwa bidii ruhu-
sa ya kutokuwepo ili aende Be-
thlehemu.[b] **29** Naye akaende-
lea kusema, 'Tafadhali niache
niende, kwa maana tuna dha-
bihu ya familia jijini, na ndugu
yangu mwenyewe ndiye aliye-
niamuru. Basi sasa, ikiwa nime-
pata kibali machoni pako, acha
niende kisirisiri, ili niwaone
ndugu zangu.' Ndiyo sababu ha-
kuja kwenye meza ya mfalme."
30 Ndipo hasira[c] ya Sauli ika-
waka juu ya Yonathani naye
akamwambia: "Wewe mwana
wa mjakazi mwasi,[d] je, mimi si-
jui vema kwamba unamchagua
mwana wa Yese, kwa aibu yako
mwenyewe na kwa aibu ya se-
hemu za siri za mama yako?[e]
31 Kwa maana siku zote amba-
zo mwana wa Yese atakuwa hai
katika nchi, wewe na ufalme
wako hutasimama imara.[f] Basi
sasa tuma watu umlete kwa-
ngu, kwa maana amekusudiwa
kufa."[g]

32 Hata hivyo, Yonathani
akamjibu Sauli baba yake na
kumwambia: "Kwa nini aua-
we?[h] Amefanya nini?"[i]
33 Ndipo Sauli akamtupia
mkuki, ili ampige;[j] na Yonatha-
ni akajua kwamba baba yake
alikuwa ameazimia kumuua
Daudi.[k] **34** Mara moja Yona-
thani akasimama kutoka meza-
ni akiwa na hasira kali,[l] naye
hakula mkate katika siku ya
pili baada ya mwezi mpya, kwa
maana alikuwa ameumizwa mo-
yoni kwa habari ya Daudi,[a] kwa
sababu baba yake mwenyewe
alikuwa amemfedhehesha.[b]

35 Na ikawa asubuhi kwa-
mba Yonathani akatoka kwe-
nda zake katika lile shamba ma-
hali alipoagana kukutana na
Daudi,[c] na mtumishi kijana ali-
kuwa pamoja naye. **36** Naye
akamwambia mtumishi wake:
"Tafadhali kimbia, tafuta ile
mishale ninayopiga."[d] Mtumi-
shi akakimbia, naye akapiga
mshale ili umpite, uende mbe-
le yake. **37** Mtumishi yule ali-
pofika mahali pa mshale ali-
okuwa amepiga Yonathani, Yo-
nathani akaanza kuita kutoka
nyuma ya mtumishi na kuse-
ma: "Je, mshale hauko mbali
zaidi na wewe?"[e] **38** Naye Yo-
nathani akaendelea kuita ku-
toka nyuma ya mtumishi:
"Upesi! Fanya haraka! Usisi-
mame tuli!" Na yule mtumishi
wa Yonathani akaiokota ile mi-
shale, kisha akarudi kwa bwa-
na wake. **39** Lakini mtumishi
huyo hakujua lolote; ila Yona-
thani na Daudi peke yao ndio
waliojua jambo hilo. **40** Ki-
sha Yonathani akampa mtumi-
shi wake silaha zake na kumwa-
mbia: "Nenda, zipeleke jijini."

41 Yule mtumishi akaenda.
Naye Daudi akasimama kutoka
hapo karibu na upande wa ku-
sini. Kisha akaanguka kifudifu-
di[f] na kuinama mara tatu; nao
wakaanza kubusiana[g] na kuli-
liana, mpaka ikawa Daudi ndi-
ye aliyelia zaidi.[h] **42** Na Yona-
thani akaendelea kumwambia
Daudi: "Nenda kwa amani,[i] kwa
maana tumeapa,[j] sisi wawili,
katika jina la Yehova, tukisema,
'Yehova na awe kati yangu na
wewe na kati ya uzao wangu na
uzao wako mpaka wakati usio
na kipimo.'"[k]

SURA 20

a Ru 4:22
1Sa 17:12
1Sa 22:7
b 1Sa 20:6
c Met 14:29
Met 22:24
d Met 15:2
Met 21:24
Efe 4:31
e 1Sa 14:50
f 1Sa 18:8
g 1Sa 19:6
Zb 79:11
Mhu 4:13
Mhu 8:4
h 1Sa 19:5
Zb 69:4
Met 17:17
Met 18:24
i Mt 27:23
Lu 23:22
j 1Sa 18:11
1Sa 19:10
Yoh 15:13
k 1Sa 20:7
l Kut 11:8
Kut 32:19
Efe 4:26

Safu ya 2

a 1Sa 18:1
b 1Sa 20:33
c 1Sa 20:19
d 1Sa 20:20
e 1Sa 20:22
f Mwa 43:28
1Sa 24:8
1Sa 25:23
2Sa 9:6
g Mwa 29:13
Mwa 45:15
1Sa 10:1
2Sa 19:39
Mdo 20:37
h 2Sa 1:26
i Hes 6:26
1Sa 1:17
Lu 7:50
Mdo 16:36
j 1Sa 20:17
1Sa 20:23
k 1Sa 20:23
1Sa 23:18
2Sa 9:7

Basi Daudi akaondoka, akaenda zake, na Yonathani akarudi jijini.

21 Baadaye Daudi akafika Nobu[a] kwa Ahimeleki[b] kuhani; naye Ahimeleki akaanza kutetemeka alipokutana na Daudi, kisha akamwambia: "Kwa nini uko peke yako, wala hakuna yeyote aliye pamoja nawe?"[c] **2** Ndipo Daudi akamwambia Ahimeleki kuhani: "Mfalme mwenyewe aliniamuru kuhusu habari fulani,[d] naye akaniambia, 'Usiache yeyote ajue lolote kuhusu habari ninayokutuma na kuhusu yale ambayo nimekuamuru.' Nami nimefanya mapatano ya kukutana mahali fulani pamoja na vijana. **3** Basi sasa, ikiwa kuna mikate mitano pamoja nawe, nipe mkononi mwangu, au chochote kinachoweza kupatikana."[e] **4** Lakini yule kuhani akamjibu Daudi na kusema: "Hakuna mkate wa kawaida mkononi mwangu, lakini kuna mkate mtakatifu;[f] ikiwa tu hao vijana wamejiepusha na wanawake."[g] **5** Kwa hiyo Daudi akamjibu kuhani na kumwambia: "Wanawake wamekaa mbali nasi kama ilivyokuwa hapo mwanzoni nilipotoka,[h] na viungo vya hao vijana vingali ni vitakatifu, ingawa utume wenyewe ni wa kawaida. Na je, si zaidi leo, mtu anapokuwa mtakatifu katika kiungo chake?" **6** Basi kuhani akampa kilicho kitakatifu,[i] kwa sababu hakukuwa na mkate mwingine hapo isipokuwa mkate wa wonyesho uliokuwa umeondolewa mbele za Yehova[j] ili kuweka mkate mpya hapo, siku ambayo uliondolewa.

7 Basi mmoja wa watumishi wa Sauli alikuwa hapo siku hiyo, akiwa amezuiliwa[a] mbele za Yehova, na jina lake lilikuwa Doegi[b] Mwedomu,[c] mkuu wa wachungaji wa Sauli.[d]

8 Na Daudi akamwambia tena Ahimeleki: "Je, hakuna chochote hapa kwako, mkuki au upanga? Kwa kuwa sikuchukua mkononi mwangu upanga wangu wala silaha zangu, kwa sababu jambo hili la mfalme lilikuwa la haraka." **9** Ndipo kuhani akasema: "Upanga wa Goliathi[e] yule Mfilisti, uliyempiga katika nchi tambarare ya chini ya Ela[f]—huu hapa, umefungwa katika nguo ya kujitanda, nyuma ya efodi.[g] Ikiwa unataka kuuchukua, uchukue, kwa sababu hakuna silaha nyingine yoyote isipokuwa upanga huu." Naye Daudi akasema tena: "Hakuna upanga mwingine kama huo. Unipe huo."

10 Kisha Daudi akaondoka, akaendelea kukimbia[h] kwa sababu ya Sauli siku hiyo, mwishowe akafika kwa Akishi mfalme wa Gathi.[i] **11** Nao watumishi wa Akishi wakaanza kumwambia: "Je, huyu si Daudi mfalme[j] wa ile nchi? Je, haikuwa kwa huyu ambaye waliendelea kuitikia kwa kucheza dansi,[k] wakisema,

> 'Sauli amepiga maelfu yake,
> Na Daudi makumi ya
> maelfu yake'?"[l]

12 Na Daudi akaanza kuyaweka maneno hayo moyoni mwake, naye akaogopa[m] sana kwa sababu ya Akishi mfalme wa Gathi. **13** Kwa hiyo akabadili[n] utimamu wake wa akili machoni pao,[o] akaanza kujifanya mwenda-wazimu mkononi mwao naye akawa akitia alama kwenye milango ya lango na kuyaacha mate yake yatiririke juu ya ndevu zake. **14** Mwishowe

SURA 21

a 1Sa 22:19
Ne 11:32
Isa 10:32
b 1Sa 22:9
c 1Sa 18:13
d Mt 10:16
e Zb 37:25
f Kut 25:30
Law 24:5
Law 24:9
Mt 12:4
Lu 6:4
g Kut 19:15
Law 15:16
2Sa 11:11
h Law 15:18
Kum 23:10
i Law 24:9
Mt 12:4
Mk 2:26
Lu 6:4
j Law 24:8

Safu ya 2

a Law 13:2
Hes 5:2
Zb 66:13
b 1Sa 22:9
Zb 52:Uta
c Mwa 36:1
Kut 12:49
Law 19:34
Kum 2:4
1Sa 14:47
d 1Sa 8:17
1Sa 11:5
1Nya 27:29
2Nya 26:10
e 1Sa 17:51
1Sa 17:54
f 1Sa 17:2
1Sa 17:50
g Kut 28:6
h 1Sa 27:1
i Yos 11:22
1Sa 5:8
1Sa 17:4
1Sa 27:2
1Fa 2:39
2Fa 12:17
Zb 56:Uta
j 1Sa 16:1
1Sa 16:13
1Sa 18:8
k 1Sa 18:6
Zb 150:4
Yer 31:4
l 1Sa 18:7
1Sa 29:5
m Zb 56:3
n Zb 34:Uta
Mt 10:16
o Zb 56:6

Akishi akawaambia watumishi
wake: "Tazameni, mtu huyu ana-
tenda kama mwenda-wazimu.
Kwa nini mmemleta kwangu?
15 Je, nimekosa watu walio na
wazimu, hivi kwamba mkamle-
ta huyu atende kiwenda-wa-
zimu mbele yangu? Je, huyu
anapaswa kuingia nyumbani
mwangu?"

22 Basi Daudi akaondoka
huko,[a] na kukimbilia[b] pa-
ngo[c] la Adulamu;[d] na ndugu
zake na nyumba yote ya baba
yake wakasikia habari hiyo,
nao wakaondoka, wakashuka
kumwendea huko. **2** Na watu
wote wenye taabu[e] na watu
wote waliokuwa na mtu anaye-
wadai deni[f] na watu wote walio-
kuwa na uchungu ndani ya
nafsi[g] wakaanza kukusanyika
pamoja kwake,[h] akawa mkuu
juu yao;[i] na watu mia nne waka-
ja kuwa pamoja naye.
3 Baadaye Daudi akaondoka
huko akaenda Mispe katika Mo-
abu, akamwambia mfalme wa
Moabu:[j] "Tafadhali, acha baba
yangu na mama[k] yangu wakae
pamoja nanyi mpaka nitakapo-
jua yale ambayo Mungu atani-
tendea." **4** Basi akawapa ma-
kao mbele ya mfalme wa Moa-
bu, nao wakaendelea kukaa pa-
moja naye siku zote ambazo
Daudi alikuwa mahali pasipo-
weza kufikiwa.[l]
5 Baada ya muda, nabii
Gadi[m] akamwambia Daudi:
"Usiendelee kukaa mahali pasi-
poweza kufikiwa. Nenda zako,
unapaswa kurudi katika nchi
ya Yuda."[n] Kwa hiyo Daudi aka-
enda zake, akaingia katika msi-
tu wa Herethi.
6 Na Sauli akasikia kwamba
Daudi na wale watu waliokuwa
pamoja naye wameonekana.
Wakati huo Sauli aliku-
wa ameketi katika Gibea chi-
ni ya mkwaju[a] ulio katika ma-
hali pa juu akiwa na mkuki[b]
wake mkononi mwake, na watu-
mishi wake wote walikuwa wa-
memzunguka. **7** Ndipo Sauli
akawaambia watumishi wake
waliokuwa wamemzunguka:
"Tafadhali, sikilizeni, enyi Wa-
benyamini. Je, mwana wa Yese[c]
atawapa ninyi nyote mashamba
na mizabibu?[d] Je, atawaweka
nyote kuwa wakuu wa maelfu[e]
na wakuu wa mamia? **8** Kwa
maana mmepanga hila, ninyi
nyote, juu yangu; wala hakuna
yeyote anayenifunulia masikio-
ni[f] mwangu wakati mwanangu
mwenyewe anapofanya agano[g]
na mwana wa Yese, wala haku-
na yeyote kati yenu anayenisi-
kitikia na kunifunulia masikio-
ni mwangu kwamba mwanangu
mwenyewe amemwinua mtumi-
shi wangu juu yangu kuwa mvi-
ziaji kama ilivyo leo hii."
9 Ndipo Doegi[h] Mwedomu,
aliyekuwa juu ya watumishi wa
Sauli, akajibu na kusema: "Ni-
limwona mwana wa Yese aki-
ja Nobu kwa Ahimeleki[i] mwana
wa Ahitubu.[j] **10** Naye akau-
liza[k] Yehova kwa ajili yake;
akampa vyakula,[l] akampa upa-
nga[m] wa Goliathi yule Mfilisti."
11 Mara moja mfalme akatuma
watu wamwite Ahimeleki mwa-
na wa Ahitubu kuhani na nyu-
mba yote ya baba yake, maku-
hani waliokuwa katika Nobu.[n]
Basi wote wakaja kwa mfalme.
12 Sasa Sauli akasema: "Ta-
fadhali, sikiliza, wewe mwa-
na wa Ahitubu!" naye akase-
ma: "Mimi hapa, bwana wa-
ngu." **13** Na Sauli akaendelea
kumwambia: "Kwa nini ni-
nyi mmepanga hila juu yangu,[o]
wewe na mwana wa Yese, kwa
kumpa yeye mkate na upanga,

SURA 22

a 1Sa 21:10
b Zb 34:19
Zb 56:13
c Zb 57:Uta
Zb 142:Uta
Ebr 11:38
d Mwa 38:1
Yos 15:35
2Sa 23:13
1Nya 11:15
Mik 1:15
e Amu 11:3
Mt 11:28
f Amo 2:6
Mt 18:26
g Amu 18:25
2Sa 17:8
h Zb 142:7
i 1Sa 30:22
2Sa 5:2
1Nya 11:15
j Ru 4:10
Ru 4:17
1Sa 14:47
1Sa 20:33
k Mwa 47:11
Kut 20:12
Met 23:24
Mt 19:19
l 1Sa 22:1
2Sa 23:13
Zb 57:1
Zb 142:Uta
m 2Sa 24:11
1Nya 21:9
1Nya 29:29
2Nya 29:25
n 1Sa 23:3

Safu ya 2

a Mwa 21:33
1Sa 31:13
1Nya 10:12
b 1Sa 18:10
1Sa 19:9
1Sa 20:33
c Ru 4:22
1Sa 20:27
1Sa 25:10
d 1Sa 8:14
e Kut 18:21
1Sa 8:12
f 1Sa 17:31
Met 15:22
g 1Sa 18:3
1Sa 20:17
h 1Sa 21:7
Zb 52:Uta
i 1Sa 21:1
j 1Sa 14:3
1Sa 22:20
k Kut 20:16
Zb 52:2
Zb 52:3
Met 19:5
Met 25:18
Met 29:12
Eze 22:9
Mt 26:59
l 1Sa 21:6
m 1Sa 21:9
n 1Sa 21:1
o Hes 35:30
Kum 19:15
1Ti 5:19

na kumuuliza Mungu kwa ajili yake, ili asimame juu yangu kama mviziaji kama ilivyo leo hii?”[a] **14** Ndipo Ahimeleki akamjibu mfalme na kusema: “Na ni nani aliye kama Daudi kati ya watumishi wako wote,[b] mwaminifu,[c] pia mwanamkwe[d] wa mfalme na mkuu juu ya walinzi wako, na mwenye kuheshimiwa nyumbani mwako?[e] **15** Je, ni leo nimeanza kumuuliza Mungu[f] kwa ajili yake? Ni jambo lisilowaziwa kwangu! Mfalme asiweke jambo lolote juu ya mtumishi wake wala juu ya nyumba nzima ya baba yangu, kwa maana, kwa habari hizi, mtumishi wako hakujua jambo lolote liwe ni kubwa au dogo.”[g]

16 Lakini mfalme akasema: “Hakika utakufa,[h] Ahimeleki, wewe pamoja na nyumba yote ya baba yako.”[i] **17** Kwa hiyo mfalme akawaambia wakimbiaji[j] waliokuwa wamesimama kumzunguka: “Geukeni, mkawaue makuhani wa Yehova, kwa sababu mkono wao pia uko pamoja na Daudi na kwa sababu walijua kwamba yeye ni mkimbizi wala hawakunifunulia habari hiyo!”[k] Lakini wale watumishi wa mfalme hawakutaka kunyoosha mkono wao ili kuwashambulia makuhani wa Yehova.[l] **18** Mwishowe mfalme akamwambia Doegi:[m] “Wewe geuka, uwashambulie makuhani!” Mara moja Doegi Mwedomu[n] akageuka yeye mwenyewe na kuwashambulia hao makuhani, na siku hiyo akawaua[o] watu 85 wenye kuvaa efodi[p] ya kitani. **19** Akapiga kwa makali ya upanga hata Nobu[q] jiji la hao makuhani, mwanamume na mwanamke vilevile, mtoto na vilevile mtoto anayenyonya na ng’ombe na punda na kondoo kwa makali ya upanga.

20 Hata hivyo, mwana mmoja wa Ahimeleki mwana wa Ahitubu, ambaye jina lake lilikuwa Abiathari,[a] akaponyoka, akakimbia amfuate Daudi. **21** Naye Abiathari akamjulisha Daudi: “Sauli amewaua makuhani wa Yehova.” **22** Ndipo Daudi akamwambia Abiathari: “Nilijua vema siku ile,[b] kwa sababu Doegi Mwedomu alikuwa hapo, kwamba bila shaka atamwambia Sauli.[c] Mimi binafsi nimeikosea kila nafsi ya nyumba ya baba yako. **23** Wewe kaa pamoja nami. Usiogope, kwa kuwa yeyote anayeitafuta nafsi yangu anaitafuta nafsi yako, kwa kuwa wewe ni mtu unayehitaji kulindwa pamoja nami.”[d]

23 Baada ya muda wakamletea Daudi habari, wakisema: “Tazama, Wafilisti wanapiga vita juu ya Keila,[e] nao wanapora viwanja vya kupuria.”[f] **2** Ndipo Daudi akamuuliza[g] Yehova, akisema: “Je, niende, na je, niwapige hawa Wafilisti?” Na Yehova akamwambia Daudi: “Nenda, nawe uwapige Wafilisti, uokoe Keila.” **3** Lakini watu wa Daudi wakamwambia: “Tazama! tunaogopa tukiwa hapa katika Yuda,[h] nasi tukienda Keila kupigana na vikosi vya Wafilisti tutaogopa hata zaidi!”[i] **4** Kwa hiyo Daudi akauliza tena kutoka kwa Yehova.[j] Sasa Yehova akamjibu na kusema: “Ondoka, shuka uende Keila, kwa sababu nitawatia Wafilisti mkononi mwako.”[k] **5** Basi Daudi akaenda pamoja na watu wake mpaka Keila, akapigana na Wafilisti na kuchukua mifugo yao, lakini akawapiga wao kwa mauaji maku-

SURA 22

a Zb 119:69
b 1Sa 19:4
1Sa 20:32
c 1Sa 24:11
1Sa 26:23
2Sa 22:23
d 1Sa 17:25
1Sa 18:27
e 1Sa 18:5
1Sa 18:13
f 1Sa 22:10
1Sa 28:6
g 1Sa 21:1
1Sa 21:2
h 1Sa 14:44
1Sa 20:31
Met 28:5
Met 28:15
i Kum 24:16
1Sa 2:32
j 1Sa 8:11
2Sa 15:1
1Fa 1:5
2Fa 10:25
k Met 28:16
Mhu 4:13
l Kut 1:17
Kum 19:10
Mdo 4:19
Mdo 5:29
m 1Sa 22:9
Zb 52:Uta
n Mwa 25:30
Mwa 36:43
Hes 24:18
2Fa 8:21
o 1Sa 2:31
2Nya 24:21
Met 29:10
p 1Sa 2:28
q 1Sa 21:1
1Sa 22:9

Safu ya 2

a 1Sa 2:31
1Sa 14:3
1Sa 23:6
1Sa 30:7
2Sa 20:25
1Fa 2:27
b 1Sa 21:7
c Met 14:15
d 1Fa 2:26

SURA 23

e Yos 15:44
1Nya 4:19
Ne 3:17
f Law 26:16
Kum 28:33
Amu 6:6
g Amu 1:1
1Sa 28:6
1Sa 30:8
2Sa 5:19
Zb 37:5
Met 3:5
h 1Sa 22:5
i 1Sa 13:5
1Sa 14:52
j Amu 6:39
k Yos 8:7
Amu 7:7
1Sa 14:6
2Sa 5:19
2Fa 3:18

bwa; na Daudi akawa mwokozi
wa wakaaji wa Keila.[a]
6 Sasa ikawa kwamba Abia-
thari[b] mwana wa Ahimeleki ali-
pokimbia kwenda kwa Daudi
kule Keila, alishuka na efodi[c]
mkononi mwake. **7** Baada ya
muda, Sauli akajulishwa: "Dau-
di amekuja Keila."[d] Naye Sauli
akaanza kusema: "Mungu ame-
muuza mkononi mwangu,[e] kwa
maana amejifungia kwa kui-
ngia katika jiji lenye milango
na mapingo." **8** Kwa hiyo Sa-
uli akawaita watu wote kwe-
nda vitani, washuke mpaka Ke-
ila, wamzingire Daudi na watu
wake. **9** Naye Daudi akaja ku-
jua kwamba Sauli alikuwa aki-
tunga madhara[f] juu yake. Basi
akamwambia Abiathari kuhani:
"Ilete efodi hapa."[g] **10** Na Da-
udi akaendelea kusema: "Ee Ye-
hova, Mungu wa Israeli,[h] mtu-
mishi wako amesikia kwa haki-
ka kwamba Sauli anatafuta
kuja Keila ili aliharibu jiji kwa
sababu yangu.[i] **11** Je, wenye
mashamba wa Keila watanitia
mkononi mwake? Je, Sauli ata-
shuka kuja kulingana na habari
ambazo mtumishi wako amesi-
kia? Ee Yehova, Mungu wa Isra-
eli, tafadhali umwambie mtumi-
shi wako." Ndipo Yehova akase-
ma: "Atashuka."[j] **12** Naye Da-
udi akaendelea kusema: "Je,
wenye mashamba wa Keila wa-
tanitia mimi na watu wangu
mkononi mwa Sauli?" Naye Ye-
hova akasema: "Watakutia."[k]
13 Mara moja Daudi akasi-
mama pamoja na watu wake,
karibu watu mia sita,[l] wakatoka
katika Keila, wakaendelea ku-
tembea mahali popote ambapo
waliweza kutembea. Naye Sauli
akajulishwa kwamba Daudi ali-
ponyoka kutoka Keila, basi aka-
acha kwenda. **14** Na Daudi
akaanza kukaa nyikani, kati-
ka mahali palipo pagumu ku-
fikiwa, naye akaendelea ku-
kaa katika eneo lenye milima katika nyika ya Zifu.[a] Na Sauli akaendelea kumtafuta sikuzote,[b] naye Mungu hakumtia mkononi mwake.[c] **15** Na Daudi akaendelea kuogopa kwa sababu Sauli alikuwa ametoka ili kuitafuta nafsi yake, Daudi alipokuwa katika nyika ya Zifu kule Horeshi.[d]
16 Sasa Yonathani mwana wa Sauli akasimama, akaenda kwa Daudi kule Horeshi, ili autie nguvu[e] mkono wake kuhusiana na Mungu.[f] **17** Naye akamwambia: "Usiogope;[g] kwa kuwa mkono wa Sauli baba yangu hautakupata, na wewe utakuwa mfalme[h] juu ya Israeli, na mimi nitakuwa wa pili kwako; na Sauli baba yangu pia anajua jambo hilo."[i] **18** Ndipo hao wawili wakafanya agano[j] mbele za Yehova; na Daudi akaendelea kukaa katika Horeshi, naye Yonathani akaenda nyumbani kwake.
19 Baadaye watu wa Zifu[k] wakaenda kwa Sauli kule Gibea,[l] wakisema: "Je, Daudi hajifichi[m] karibu nasi katika mahali palipo pagumu kufikiwa kule Horeshi,[n] katika kilima cha Hakila,[o] kilicho upande wa kuume wa Yeshimoni?[p] **20** Basi sasa, kulingana na tamaa yote ya nafsi yako[q] ya kushuka, Ee mfalme, shuka, na sehemu yetu itakuwa ni kumtia yeye mkononi mwa mfalme."[r] **21** Ndipo Sauli akasema: "Ninyi ni wabarikiwa wa Yehova,[s] kwa maana mmenihurumia. **22** Tafadhali nendeni, vumilieni tena kidogo tu, mhakikishe na mwone mahali pake ambapo mguu wake

SURA 23
a 1Sa 22:5
1Sa 23:1
b 1Sa 22:20
c Kut 28:30
1Sa 14:3
d 1Sa 23:1
e Kut 15:9
1Sa 23:14
Zb 71:11
f Met 12:20
Met 14:22
Met 16:30
Met 24:8
g Hes 27:21
1Sa 30:7
h Zb 17:6
Zb 50:15
Yer 33:3
i 1Sa 22:19
Met 28:15
j Zb 118:21
k Zb 31:8
Zb 62:2
Zb 94:11
Zb 118:8
l 1Sa 22:2
1Sa 25:13
1Sa 30:9

Safu ya 2
a Yos 15:55
1Sa 23:24
1Sa 26:1
1Nya 2:42
Zb 54:Uta
b 1Sa 18:29
1Sa 20:33
1Sa 27:1
Zb 54:3
c 1Sa 2:9
Zb 33:18
Zb 54:4
Zb 124:7
Met 21:30
Ro 8:31
d 1Sa 23:18
e Kum 3:28
Ne 2:18
Ayu 16:5
Met 17:17
Met 27:9
Lu 22:32
Mdo 15:32
Ebr 10:25
f Zb 37:5
1Pe 5:7
g Zb 27:1
Isa 41:10
h 1Sa 16:13
2Sa 2:4
2Sa 5:3
i 1Sa 20:31
1Sa 24:20
j 1Sa 18:3
1Sa 20:42
1Sa 22:8
2Sa 21:7
k 1Nya 2:42
l 1Sa 10:26
1Sa 15:34
m 1Sa 22:17
1Sa 26:1
Zb 54:Uta
n 1Sa 23:15
o 1Sa 26:3
p 1Sa 23:24
1Sa 26:1
q 1Sa 18:29
1Sa 20:33
Zb 112:10
Met 11:23
r Zb 54:3
Zb 70:2
Met 29:26
s Amu 17:2

utakuja—yeyote aliyemwona
hapo—kwa maana nimeambi-
wa kwamba bila shaka yeye ni
mjanja.[a] **23** Angalieni na ku-
hakikisha kuhusu mahali pote
pa kujificha ambapo yeye hujifi-
cha; nanyi mrudi kwangu mki-
wa na huo ushuhuda, nami ni-
taenda pamoja nanyi; na itatu-
kia kwamba, ikiwa yupo katika
nchi hiyo, nitamtafuta kwa ua-
ngalifu kati ya maelfu[b] yote ya
Yuda."

24 Kwa hiyo wakaondoka,
wakaenda Zifu[c] kumtangulia
Sauli, huku Daudi na watu wake
wakiwa katika nyika ya Maoni[d]
katika Araba[e] upande wa ku-
sini wa Yeshimoni. **25** Baada-
ye Sauli akaja na watu wake
kumtafuta.[f] Walipomjulisha
Daudi, mara moja akashuka
kwenda kwenye mwamba,[g] naye
akaendelea kukaa katika nyika
ya Maoni. Sauli aliposikia ha-
bari hiyo, akaenda kumfuatili-
a[h] Daudi katika nyika ya Ma-
oni. **26** Mwishowe Sauli akaja
upande huu wa mlima, na Dau-
di na watu wake wakawa upa-
nde mwingine wa mlima huo.
Basi Daudi akafanya haraka
kuondoka[i] kwa sababu ya Sau-
li; wakati huo wote Sauli na
watu wake walikuwa wakimzu-
nguka Daudi na watu wake ili
kuwakamata.[j] **27** Lakini mju-
mbe fulani akamjia Sauli, akise-
ma: "Fanya haraka uende, kwa
maana Wafilisti wameivamia
nchi!" **28** Ndipo Sauli akage-
uka, akaacha kumfuatilia Dau-
di,[k] akaenda kukutana na Wa-
filisti. Ndiyo sababu wamepaita
mahali hapo Mwamba wa Miga-
wanyiko.

29 Ndipo Daudi akapanda
kutoka huko, akaenda kukaa
katika mahali palipo pagumu
kufikiwa kule En-gedi.[l]

SURA 23
a Mt 10:16
b Yos 22:30
1Sa 10:19
c 1Sa 23:14
d Yos 15:55
1Sa 25:2
e Kum 1:7
f 1Sa 26:2
Zb 54:3
g 1Sa 23:28
h Met 11:19
i 1Sa 19:12
2Sa 15:14
Zb 31:22
j 2Nya 20:12
Zb 17:9
2Ko 1:8
k 2Sa 22:1
Zb 18:Uta
Zb 18:2
Zb 54:7
l Yos 15:62
2Nya 20:2
Wim 1:14
Eze 47:10

Safu ya 2

SURA 24
a 1Sa 23:28
b 1Sa 23:29
c 1Sa 13:2
d Zb 37:32
Zb 38:12
e Zb 104:18
f Kum 23:13
Amu 3:24
1Fa 18:27
g Zb 57:Uta
Zb 142:Uta
h 1Sa 26:8
1Sa 26:23
i Met 24:29
Mt 7:12
j 2Sa 24:10
Ro 2:15
1Yo 3:20
k 1Sa 26:11
2Sa 1:14
l Kut 22:28
1Nya 16:22
Zb 105:15
Mdo 23:5
m Law 19:18
Zb 7:4
Mt 5:44
Ro 12:17
Ro 12:19
Ro 12:21

24 Na ikawa kwamba mara
tu Sauli aliporudi baa-
da ya kuwafuatilia Wafilisti,[a]
wakamletea habari, wakisema:
"Tazama! Daudi yuko katika
nyika ya En-gedi."[b]

2 Na Sauli akachukua watu
elfu tatu waliochaguliwa[c] ku-
toka katika Israeli yote kwe-
nda kumtafuta Daudi[d] na
watu wake juu ya miamba iliyo
wazi ya mbuzi wa milimani.[e]
3 Mwishowe akafika kwenye
mazizi ya mawe ya kondoo ka-
ndo ya barabara, mahali amba-
po palikuwa na pango. Basi
Sauli akaingia ndani kwenda
haja,[f] huku Daudi na watu wake
wakiwa katika sehemu za nyu-
ma kabisa za pango hilo,[g] wa-
kiwa wameketi. **4** Na watu
wa Daudi wakaanza kumwa-
mbia: "Hii ndiyo siku amba-
yo Yehova anakuambia, 'Ta-
zama! Ninamtia adui yako mko-
noni mwako,[h] nawe umtendee
kama inavyoonekana vema ma-
choni pako.'"[i] Kwa hiyo Dau-
di akasimama, akakata kimya-
kimya upindo wa koti lisilo na
mikono la Sauli. **5** Lakini baa-
daye moyo wa Daudi ukaen-
delea kumchoma[j] kwa saba-
bu alikuwa amekata upindo
wa lile koti la Sauli. **6** Basi
akawaambia watu wake: "Ni ja-
mbo lisilowaziwa kwangu, kwa
maoni ya Yehova, kwamba ni-
mfanyie bwana wangu jambo
hili, mtiwa-mafuta[k] wa Yeho-
va, kwa kunyoosha mkono wa-
ngu juu yake, kwa kuwa yeye
ni mtiwa-mafuta wa Yehova."[l]
7 Kwa hiyo Daudi akawatawa-
nya watu wake kwa maneno
hayo, naye hakuwaruhusu wa-
mshambulie Sauli.[m] Naye Sauli
akainuka kutoka katika lile pa-
ngo na kwenda zake.

8 Basi Daudi akainuka baada-

ye, akatoka nje ya lile pango na
kumwita Sauli, akisema: "Bwana wangu[a] mfalme!" Ndipo Sau-
li akatazama nyuma, naye Dau-
di akainama kifudifudi,[b] aka-
sujudu. **9** Na Daudi akaende-
lea kumwambia Sauli: "Kwa nini
unayasikiliza maneno ya watu,[c]
wakisema, 'Tazama! Daudi ana-
tafuta kukudhuru'? **10** Taza-
ma, leo macho yako yameona ji-
nsi Yehova alivyokutia leo mko-
noni mwangu ndani ya pango;
na mtu fulani alisema nikuue,[d]
lakini nikakusikitikia, nikasema,
'Sitanyoosha mkono wangu
juu ya bwana wangu, kwa maana
yeye ni mtiwa-mafuta[e] wa Yeho-
va.' **11** Basi ona baba yangu,[f]
ndiyo, ona mkononi mwangu
upindo wa koti lako lisilo na
mikono, kwa sababu nilipokata
upindo wa koti lako, sikuku-
ua. Ujue na kuona kwamba ha-
kuna ubaya[g] wowote wala ma-
asi mkononi mwangu, nami si-
kutenda dhambi juu yako,
huku wewe ukiivizia nafsi yangu
ili kuiondolea mbali.[h] **12** Ye-
hova na ahukumu kati yangu
na wewe;[i] na Yehova anilipizie
kisasi[j] kutoka kwako, lakini
mkono wangu mwenyewe hauta-
kuja juu yako.[k] **13** Kama vile
inavyosema methali ya watu
wa kale, 'Katika waovu uovu
utatoka,'[l] lakini mkono wangu
mwenyewe hautakuja juu yako.
14 Je, mfalme wa Israeli ameto-
ka nje kufuata nani? Unamfua-
tilia nani? Mbwa aliyekufa?[m] Ki-
roboto mmoja?[n] **15** Na Yehova
atakuwa mwamuzi, naye atahu-
kumu kati yangu na wewe, naye
ataona na kufanya kesi[o] kwa ajili
yangu na kunihukumu ili ku-
niweka huru kutoka mkononi
mwako."

16 Na ikawa kwamba, mara
tu Daudi alipomaliza kumwa-
mbia Sauli maneno hayo, Sauli
akasema: "Je, hii ni sauti yako,
Daudi mwanangu?"[a] Naye Sau-
li akapaaza sauti yake, akalia.[b]
17 Naye akamwambia Daudi:
"Wewe ni mwadilifu kuliko
mimi,[c] kwa maana wewe ndiye
umenitendea mema,[d] nami ndiye
nimekutendea uovu. **18** Nawe
umefunua leo mema ambayo
umenitendea kwa maana Yeho-
va alinitia mkononi mwako,[e]
nawe hukuniua. **19** Kwa maa-
na, mtu akimpata adui yake,
je, atamwacha ashike njia ae-
nde zake salama?[f] Basi Yeho-
va mwenyewe atakupa thawabu
ya mema,[g] kwa kuwa leo ume-
nitendea hivyo. **20** Na sasa ta-
zama! Najua vema bila shaka
kwamba wewe utatawala ukiwa
mfalme,[h] na kwamba ufa-
lme wa Israeli utadumu mko-
noni mwako. **21** Basi sasa nia-
pie kwa Yehova[i] kwamba hu-
taukatilia mbali uzao wangu
baada yangu na kwamba hutali-
angamiza jina langu kutoka ka-
tika nyumba ya baba yangu."[j]
22 Kwa hiyo Daudi akamwapia
Sauli, kisha Sauli akaenda
nyumbani kwake.[k] Naye Daudi
na watu wake wakapanda, waka-
enda mahali palipo pagumu
kufikiwa.[l]

25 Baadaye Samweli[m] aka-
fa; na Israeli wote waka-
kusanyika pamoja, wakamwo-
mbolezea[n] na kumzika karibu
na nyumba yake huko Rama.[o]
Kisha Daudi akaondoka, aka-
shuka kwenda katika nyika ya
Parani.[p]

2 Sasa palikuwa na mtu fula-
ni katika Maoni,[q] na kazi yake
ilikuwa katika Karmeli.[r] Na mtu

SURA 24

a 1Sa 26:17
b 1Sa 20:41
1Sa 25:23
Ro 12:10
Ro 13:7
c Law 19:16
1Sa 26:19
Zb 101:5
Met 16:28
Met 17:4
d 1Sa 24:4
e 1Sa 9:16
1Sa 10:1
1Sa 26:9
Zb 105:15
f 1Sa 18:27
1Sa 22:14
Met 15:1
Met 25:15
g 1Sa 26:18
Zb 7:3
Zb 35:7
h 1Sa 23:14
Zb 140:1
i 1Sa 26:23
Zb 7:8
j Kum 32:35
Zb 94:1
Nah 1:2
Ro 12:19
Ebr 10:30
k 1Sa 26:11
l Mwa 4:7
Met 11:5
Mt 7:17
Ga 6:7
m 1Sa 17:43
2Sa 9:8
Met 22:4
Mt 23:12
n 1Sa 26:20
o Zb 35:1
Zb 43:1
Zb 119:154
Mik 7:9

Safu ya 2

a 1Sa 26:17
b Mwa 27:38
c 1Sa 26:21
d Met 25:21
Ro 12:17
e 1Sa 24:4
1Sa 24:10
1Sa 26:8
f Mt 5:44
Ro 12:17
g 1Sa 26:25
2Nya 16:9
Zb 18:20
h 1Sa 13:14
1Sa 15:28
1Sa 18:8
1Sa 20:31
1Sa 23:17
i Law 19:12
Kum 6:13
j 2Sa 9:1
2Sa 21:7
k 1Sa 15:34
l 1Sa 23:29
Met 14:15
Mt 10:16

SURA 25

m 1Sa 1:20
1Sa 2:18
1Sa 3:20
Zb 99:6

n Hes 20:29; Kum 34:8; Mdo 8:2; o 1Sa 7:17; 1Sa 28:3; p Mwa 21:21; Hes 13:26; q 1Sa 23:24; r Yos 15:1; Yos 15:48; Yos 15:55.

huyo alikuwa mkuu sana, naye
alikuwa na kondoo elfu tatu na
mbuzi elfu moja; naye alikuwa
na kazi ya kukata[a] kondoo zake
manyoya kule Karmeli. **3** Na
jina la mtu huyo lilikuwa Naba-
li,[b] na jina la mke wake lilikuwa
Abigaili.[c] Naye mke huyo ali-
kuwa mwenye busara[d] njema
na mrembo wa umbo, lakini
mume alikuwa mkali na mwe-
nye matendo mabaya;[e] naye ali-
kuwa Mkalebu.[f] **4** Basi Dau-
di akasikia akiwa nyikani kwa-
mba Nabali alikuwa akikata ko-
ndoo zake manyoya.[g] **5** Kwa
hiyo Daudi akatuma wanau-
me kumi vijana, na Daudi aka-
waambia hao vijana: "Pande-
ni, mwende Karmeli, mfike kwa
Nabali, mkamuulize kwa jina la-
ngu kuhusu hali yake.[h] **6** Na-
nyi mkamwambie ndugu yangu
hivi, 'Wema uwe kwako[i] na pia
wema uwe kwa nyumba yako
na wema uwe kwa vyote ulivyo
navyo. **7** Na sasa nimesikia
kwamba una wakataji-manyo-
ya. Sasa wachungaji wako wali-
kuwa pamoja nasi.[j] Hatukuwa-
sumbua,[k] wala hakuna chocho-
te chao ambacho kilipotea siku
zote walizokuwa katika Karme-
li. **8** Waulize hao vijana wako,
nao watakuambia, ndipo vija-
na wangu wapate kibali macho-
ni pako, kwa kuwa tumekuja
siku nzuri. Tafadhali, wape wa-
tumishi wako na Daudi mwana
wako chochote ambacho mko-
no wako unaweza kupata.'"[l]
9 Basi wale vijana wa Daudi
wakaja na kumwambia Nabali
kulingana na maneno hayo yote
katika jina la Daudi na kisha
wakangoja. **10** Lakini Nabali
akawajibu watumishi wa Dau-
di na kusema: "Daudi ni nani,[m]
na mwana wa Yese ni nani?
Siku hizi watumishi wanaoto-
roka, kila mmoja kutoka mbe-
le ya bwana wake, wamekuwa
wengi.[a] **11** Na je, nichukue
mkate[b] wangu na maji yangu
na nyama yangu ambayo ni-
mewachinjia wakataji-manyoya
wangu na kuwapa watu ambao
sijui hata wanatoka wapi?"[c]
12 Kwa hiyo vijana wa Dau-
di wakageuka, wakarudi, wa-
kamletea habari kulingana na
maneno hayo yote. **13** Mara
hiyo Daudi akawaambia watu
wake: "Kila mtu ajifunge upa-
nga wake!"[d] Basi kila mtu akaji-
funga upanga wake na pia Daudi
akajifunga upanga wake; waka-
anza kupanda nyuma ya Daudi,
karibu watu mia nne, huku mia
mbili wakibaki kando ya mizigo.[e]
14 Na wakati huohuo, mmo-
ja wa vijana akaleta habari
kwa Abigaili, mke wa Naba-
li, akisema: "Tazama! Daudi
alituma wajumbe kutoka nyi-
kani ili kumtakia bwana wetu
mema, lakini akawakemea kwa
sauti kali.[f] **15** Na watu hao
walikuwa wema sana kwetu,
nao hawakutusumbua, nasi ha-
tukupoteza hata kitu kimo-
ja siku zote za kutembea kwe-
tu tukiwa shambani.[g] **16** Wa-
likuwa ukuta[h] kutuzunguka
wakati wa usiku na wakati wa
mchana, siku zote tulipoku-
wa pamoja nao, tukichunga ku-
ndi. **17** Na sasa ujue na kuona
jambo la kufanya, kwa maana
msiba umeazimiwa[i] juu ya bwa-
na wetu na juu ya nyumba yake
yote, kwa maana yeye ni mtu
asiyefaa kitu[j] sana hata mtu ha-
wezi kusema naye."
18 Mara moja Abigaili[k] aka-
fanya haraka, akachukua mika-
te mia mbili na mitungi miwi-
li mikubwa ya divai[l] na kondoo
watano[m] na vipimo vitano vya
sea vya nafaka iliyochomwa[n] na

SURA 25

a 2Sa 13:23
b 1Sa 25:25
1Sa 25:38
c 1Sa 27:3
1Sa 30:5
d Met 14:1
Met 24:3
Met 31:26
e 1Sa 25:17
1Sa 25:21
Isa 32:5
f Hes 13:6
Hes 32:12
g 2Sa 13:23
h 1Sa 17:22
i Mt 10:12
Lu 10:5
j 1Sa 22:2
k 1Sa 25:15
Lu 3:14
l Kum 15:7
Met 3:27
Lu 11:41
Mdo 20:35
Ebr 13:16
m Kut 5:2
Zb 123:4

Safu ya 2

a 1Sa 22:2
Isa 32:6
b Kum 8:17
Amu 8:6
2Ko 9:10
c Met 21:13
Mhu 9:15
Isa 32:6
Lu 6:38
Yak 2:16
d Zb 37:8
Met 15:1
Mhu 7:9
e 1Sa 10:22
1Sa 17:22
1Sa 30:24
f 1Sa 25:10
2Sa 16:7
g 1Sa 25:7
h 1Sa 23:1
Ayu 1:10
Met 18:11
i 1Sa 20:9
1Sa 25:13
Est 7:7
j 1Sa 25:3
2Nya 13:7
Isa 32:7
k 1Sa 25:3
1Sa 25:23
1Sa 25:32
l Mwa 32:13
m 2Sa 17:29
n Ru 2:14
1Sa 17:17
2Sa 17:28

keki mia moja za zabibu kavu[a]
na keki mia mbili za tini zi-
lizoshinikizwa,[b] akazipakia juu
ya punda. **19** Kisha akawaam-
bia vijana wake: "Piteni mbe-
le yangu.[c] Tazama! Naja nyu-
ma yenu." Lakini hakumwa-
mbia Nabali mume wake jambo
lolote.

20 Na ikatukia kwamba ali-
pokuwa amempanda punda[d] na
kushuka kwenye mlima kisiri,
tazama, kumbe, Daudi na watu
wake walikuwa wakishuka kuja
kukutana naye. Basi akakuta-
na nao. **21** Naye Daudi aliku-
wa amesema: "Ni kwa ajili ya
kukatishwa tamaa tu kwamba
nililinda kila kitu cha mtu huyu
nyikani wala hakuna hata kitu
kimoja kati ya vyote vilivyo
vyake ambacho kilipotea,[e] na
bado ananilipa uovu kwa ajili
ya wema.[f] **22** Basi Mungu na
awafanyie hivyo adui za Dau-
di na kuzidisha[g] ikiwa nitaacha
abaki kufikia asubuhi[h] yeyote
kati ya wote walio wake anaye-
kojoa ukutani."[i]

23 Abigaili alipomwona Dau-
di, akafanya haraka mara moja,
akashuka kutoka juu ya yule
punda, akaanguka kifudifudi
mbele ya Daudi, akainama[j] chi-
ni. **24** Kisha akaanguka mi-
guuni pake[k] na kusema: "Kosa
na liwe juu yangu mwenyewe,[l]
Ee bwana wangu; na, tafadha-
li mwache kijakazi wako aseme
masikioni mwako,[m] nawe uyasi-
kilize maneno ya kijakazi wako.
25 Tafadhali, bwana wangu asi-
weke moyo wake juu ya mtu
huyu asiyefaa kitu,[n] Nabali,
kwa maana, kama lilivyo jina
lake, ndivyo alivyo yeye. Nabali
ndilo jina lake, na ukosefu wake
wa akili uko pamoja naye.[o] La-
kini mimi kijakazi wako, si-
kuwaona wale vijana wa bwa-
na wangu uliokuwa umewatu-
ma. **26** Basi sasa, bwana wa-
ngu, kama anavyoishi Yehova[a]
na kama inavyoishi nafsi yako,[b]
Yehova amekuzuia[c] usiingie ka-
tika hatia ya damu[d] na kufa-
nya mkono wako mwenyewe
ukuokoe.[e] Basi sasa adui zako
na wale wanaotafuta kumdhu-
ru bwana wangu na wawe kama
Nabali.[f] **27** Na sasa zawadi
hii ya baraka[g] ambayo kijaka-
zi wako amemletea bwana wa-
ngu, ipewe wale vijana wanao-
tembea katika hatua[h] za bwa-
na wangu. **28** Tafadhali, sa-
mehe makosa ya kijakazi wako,[i]
kwa maana bila shaka Yehova
atamfanyia bwana wangu nyu-
mba inayodumu,[j] kwa maana
bwana wangu anapigana vita
vya Yehova;[k] na ubaya hauta-
patikana ndani yako siku zako
zote.[l] **29** Wakati mwanadamu
atakaposimama ili kukufuatilia
na kuitafuta nafsi yako, nafsi
ya bwana wangu itakuwa ime-
fungwa katika mfuko wa uzima[m]
pamoja na Yehova Mungu
wako;[n] lakini nafsi ya adui zako
yeye ataitupa mbali kama kuto-
ka ndani ya tundu la kombeo.[o]
30 Na itatukia kwamba, kwa
kuwa Yehova atamfanyia bwa-
na wangu mema kukuelekea
kulingana na yote ambayo ame-
sema, hakika atakuweka kuwa
kiongozi juu ya Israeli.[p] **31** Na
usiache hili liwe kwako saba-
bu ya kufadhaika wala kikwazo
kwa moyo wa bwana wangu,
kwa kumwaga damu bila saba-
bu[q] na pia kwa kuacha mko-
no wa bwana wangu mwenye-
we umwokoe.[r] Na hakika Ye-
hova atamfanyia mema bwa-
na wangu, nawe utamkumbuka[s]
kijakazi wako."

SURA 25

a 1Sa 30:12
2Sa 16:1
b 1Nya 12:40
Met 25:21
Met 25:22
c Mwa 32:16
d Yos 15:18
2Fa 4:24
e 1Sa 25:7
f 1Sa 25:10
Zb 35:12
Zb 38:20
Zb 109:5
Met 17:13
g Ru 1:17
1Sa 3:17
1Sa 14:44
1Sa 20:13
2Sa 3:9
h Met 12:16
Met 14:17
Met 26:4
Ro 12:21
i 1Fa 14:10
1Fa 16:11
1Fa 21:21
2Fa 9:8
2Fa 10:7
j 1Sa 24:8
1Sa 25:41
k 2Fa 4:37
Est 8:3
l 2Sa 14:9
m Mwa 44:18
2Sa 14:12
n 1Sa 25:17
o Isa 32:6

Safu ya 2

a 1Sa 20:21
1Fa 2:24
b 1Sa 1:26
2Sa 14:19
2Fa 2:2
c Mwa 20:6
Mt 6:13
d Mwa 9:6
Hes 35:30
e Ro 12:19
f 1Sa 25:25
Yer 29:22
g Mwa 33:11
1Sa 25:18
1Sa 30:26
2Fa 5:15
Met 18:16
Met 25:21
Met 25:22
h 1Sa 22:2
i Met 18:12
Met 22:4
j 1Sa 15:28
2Sa 7:11
1Fa 9:5
k 1Sa 17:45
1Sa 18:17
2Sa 5:2
l 1Sa 24:11
1Fa 15:5
Zb 119:1
m Zb 41:2
n Mwa 15:1
Kum 33:29
Zb 66:9
o Yer 10:18
p 1Sa 13:14
1Sa 15:28
1Sa 23:17
2Sa 6:21
2Sa 7:8
1Nya 17:7
Zb 89:20
q 1Sa 25:26
Efe 4:26

r Kum 32:35; 1Sa 24:15; Zb 94:1; Ro 12:19; s Mwa 40:14.

32 Ndipo Daudi akamwambia Abigaili: "Abarikiwe Yehova Mungu wa Israeli,[a] aliyekutuma leo unipokee! **33** Busara yako na ibarikiwe,[b] nawe ubarikiwe, ambaye umenizuia leo nisiingie katika hatia ya damu[c] na kuacha mkono wangu mwenyewe uniokoe.[d] **34** Na, kwa upande mwingine, kama anavyoishi Yehova Mungu wa Israeli, ambaye amenizuia nisikudhuru wewe,[e] kama hungelifanya haraka ili uje kunipokea,[f] kufikia wakati wa nuru ya asubuhi hangelibaki kwa Nabali mtu yeyote anayekojoa ukutani."[g] **35** Kwa hiyo Daudi akapokea kutoka mkononi mwake vitu ambavyo alikuwa amemletea, naye akamwambia: "Panda uende kwa amani[h] nyumbani kwako. Tazama, nimeisikiliza sauti yako na kukufikiria[i] wewe."

36 Baadaye Abigaili akaingia kwa Nabali, na tazama, mwanamume huyo alikuwa akifanya karamu katika nyumba yake, karamu kama ile ya mfalme;[j] na moyo wa Nabali ulikuwa ukichangamka ndani yake, naye alikuwa amelewa[k] kabisa; na kufikia nuru ya asubuhi mke hakuweza kumwambia jambo lolote, liwe ni dogo au kubwa. **37** Na ikawa kwamba asubuhi, divai ilipokuwa imemtoka Nabali, mke wake akamwambia mambo hayo yote. Na moyo[l] wa mwanamume huyo ukafa ndani yake, naye akawa kama jiwe. **38** Baada ya hapo karibu siku kumi zikapita, ndipo Yehova akampiga[m] Nabali, naye akafa.

39 Basi Daudi akasikia kwamba Nabali amekufa, kwa hiyo akasema: "Abarikiwe Yehova, ambaye amefanya kesi[n] ya shutuma[o] yangu ili kuniweka huru kutoka mkononi mwa Nabali na ambaye amemzuia mtumishi wake asifanye ubaya,[a] na Yehova ameurudisha ubaya wa Nabali juu ya kichwa chake mwenyewe!"[b] Kisha Daudi akatuma watu na kumwambia Abigaili kwamba alipenda kumchukua awe mke wake.[c] **40** Basi watumishi wa Daudi wakamjia Abigaili kule Karmeli na kumwambia hivi: "Daudi ametutuma kwako tukuchukue uwe mke wake." **41** Mara moja akasimama, akainama kifudifudi,[d] akasema: "Tazama, mimi ni kijakazi wako, niwe mjakazi wa kuosha miguu[e] ya watumishi wa bwana wangu."[f] **42** Kisha Abigaili[g] akafanya haraka, akaondoka, akapanda punda[h] pamoja na wanawali wake watano wakiwa wanatembea nyuma yake; akaenda pamoja na wajumbe wa Daudi, na kisha akawa mke wake.

43 Daudi pia alikuwa amemchukua Ahinoamu[i] kutoka Yezreeli;[j] na hao wanawake wawili wakaja kuwa wake zake.[k]

44 Lakini Sauli alikuwa amemkabidhi Mikali[l] binti yake, mke wa Daudi, kwa Palti[m] mwana wa Laishi, aliyetoka Galimu.[n]

26 Baada ya muda watu wa Zifu[o] wakamjia Sauli kule Gibea,[p] wakisema: "Je, Daudi hajifichi katika kilima cha Hakila,[q] kinachoelekeana na Yeshimoni?"[r] **2** Naye Sauli akaondoka,[s] akashuka, akaenda katika nyika ya Zifu, na watu elfu tatu[t] walikuwa pamoja naye, watu waliochaguliwa wa Israeli, kumtafuta Daudi katika nyika ya Zifu. **3** Na Sauli akapiga kambi katika kili-

SURA 25
a Zb 41:13; Zb 72:18
b Zb 141:5; Met 9:9; Met 25:12
c Kum 19:10; 1Sa 25:26; Zb 73:2; Met 15:1; Yak 5:20
d 1Sa 25:31; Zb 56:13; Ro 12:19
e 1Sa 25:24
f 1Sa 25:18; Met 29:8
g 1Sa 25:22
h 1Sa 20:42; 2Sa 15:9; 2Fa 5:19
i Mwa 19:21; Met 28:23
j 2Sa 13:23; 1Fa 4:22; Est 1:5
k 1Fa 20:16; Met 20:1; Ho 4:11; 1Ko 6:10; Efe 5:18
l Kum 28:28; Zb 102:4; Zb 143:4
m Mwa 38:7; Mwa 38:10; 2Sa 6:7; 2Fa 19:35; Mdo 12:23
n Kum 32:35; 1Sa 24:15; Zb 35:1; Zb 43:1; Met 22:23
o 1Sa 25:10; 1Sa 25:14

Safu ya 2
a 1Sa 25:34
b Amu 9:57; 1Fa 2:44; Zb 7:16
c Met 18:22; Met 31:10; Met 31:31
d Ru 2:10
e Mwa 18:4; Lu 7:44; Yoh 13:5; 1Ti 5:10
f Met 15:33; Met 18:12
g 1Sa 25:3
h Mwa 24:61
i 1Sa 27:3; 2Sa 3:2; 1Nya 3:1
j Yos 15:56
k 1Sa 30:5; 2Sa 5:13; 2Sa 12:8
l 1Sa 18:20
m 2Sa 3:15
n Isa 10:30

SURA 26
o Yos 15:55; 1Sa 23:14; Zb 54:Uta
p Amu 19:14; 1Sa 10:26; 1Sa 11:4

q 1Sa 23:19; r 1Sa 23:24; s 1Sa 23:23; 1Sa 24:17; t 1Sa 24:2.

ma cha Hakila, kinachoelekeana na Yeshimoni, kando ya barabara, naye Daudi alikuwa akikaa nyikani. Naye akaona kwamba Sauli amemfuata nyikani.
4 Basi Daudi akatuma wapelelezi[a] ili ajue kama kweli Sauli amekuja. **5** Baadaye Daudi akasimama, akaenda mahali ambapo Sauli alikuwa amepiga kambi, na Daudi akaona mahali ambapo Sauli alikuwa amelala, na pia Abneri[b] mwana wa Neri mkuu wa jeshi lake; na Sauli alikuwa amelala katika uwanja wa kambi,[c] watu wakiwa wamepiga kambi kumzunguka. **6** Ndipo Daudi akamwambia Ahimeleki Mhiti,[d] na Abishai[e] mwana wa Seruya,[f] ndugu ya Yoabu: "Ni nani atakayeshuka aende pamoja nami kwa Sauli kambini?" Naye Abishai akasema: "Mimi nitashuka pamoja nawe."[g] **7** Na Daudi akaondoka pamoja na Abishai kwenda kwa wale watu wakati wa usiku; na tazama! Sauli alikuwa amelala katika uwanja wa kambi, huku mkuki wake ukiwa umechomekwa chini penye kichwa chake, na Abneri na watu walikuwa wamelala kumzunguka.

8 Sasa Abishai akamwambia Daudi: "Mungu leo amemtia adui yako mkononi mwako.[h] Tafadhali sasa, acha nimpigilie chini kwa mkuki mara moja tu, nami sitafanya hivyo mara mbili." **9** Hata hivyo, Daudi akamwambia Abishai: "Usimwangamize, kwani ni nani amepata kunyoosha mkono wake juu ya mtiwa-mafuta wa Yehova,[i] naye akabaki bila hatia?"[j]
10 Na Daudi akasema tena: "Kama Yehova anavyoishi,[k] Yehova mwenyewe atampiga;[l] au siku yake itakuja[m] naye atakufa, au ataanguka vitani,[n] na kufagiliwa mbali.[a] **11** Ni jambo lisilowaziwa[b] kwangu, kwa maoni ya Yehova,[c] kwamba ninyooshe mkono wangu[d] juu ya mtiwa-mafuta wa Yehova![e] Kwa hiyo, tafadhali sasa, chukua mkuki ulio karibu na kichwa chake na lile gudulia la maji, nasi twende zetu." **12** Basi Daudi akachukua ule mkuki na lile gudulia la maji kutoka pale karibu na kichwa cha Sauli, kisha wakaondoka; na hakuna yeyote aliyeona[f] wala yeyote aliyeangalia wala yeyote aliyeamka, kwa maana wote walikuwa wamelala, kwa sababu walikuwa wameshikwa na usingizi mzito[g] kutoka kwa Yehova. **13** Ndipo Daudi akapita, akaenda upande ule mwingine, akasimama kwenye kilele cha mlima akiwa umbali fulani, nafasi iliyokuwa kati yao ilikuwa ni kubwa.

14 Naye Daudi akaanza kuwaita watu na Abneri mwana wa Neri, akisema: "Je, hutajibu, Abneri?" Kwa hiyo Abneri[h] akajibu na kusema: "Wewe ni nani ambaye umemwita mfalme?"
15 Na Daudi akaendelea kumwambia Abneri: "Je, wewe si mwanamume? Na ni nani aliye kama wewe katika Israeli? Kwa nini, basi, hukumlinda bwana wako mfalme? Kwa sababu mmoja wa watu aliingia ili kumwangamiza mfalme bwana wako.[i] **16** Jambo hili ambalo umefanya si jema. Kama Yehova anavyoishi,[j] ninyi mnastahili kufa,[k] kwa sababu hamkumlinda[l] bwana wenu, mtiwa-mafuta wa Yehova.[m] Na sasa ona mahali ulipo mkuki wa mfalme na gudulia la maji[n] vilivyokuwa karibu na kichwa chake."

17 Naye Sauli akaanza kutambua sauti ya Daudi na kusema: "Je, hii ni sauti yako,

SURA 26
a Yos 2:1
Mt 10:16
b 1Sa 14:50
1Sa 17:55
2Sa 2:8
2Sa 3:27
c 1Sa 17:20
d Mwa 10:15
Mwa 15:20
e 2Sa 16:9
2Sa 18:5
f 2Sa 2:18
2Sa 23:18
1Nya 2:16
g Amu 7:10
1Sa 14:7
h 1Sa 24:4
1Sa 26:23
i 1Sa 10:1
1Sa 24:6
2Sa 1:14
j 1Nya 16:22
Zb 20:6
Zb 105:15
Lu 18:7
k 1Sa 20:21
1Sa 25:26
l Kum 32:35
1Sa 24:12
1Sa 25:38
Zb 94:1
Zb 94:23
Ro 12:19
Yud 9
m Ayu 14:5
Zb 37:13
Zb 90:10
Mhu 8:13
n 1Sa 31:3
1Sa 31:6

Safu ya 2
a 1Sa 12:25
b 1Sa 14:45
1Sa 24:6
c Zb 40:8
Zb 119:97
d Law 19:18
Met 24:29
Ro 12:17
e 1Nya 16:22
Zb 20:6
Zb 105:15
f 1Sa 24:4
g Mwa 2:21
Mwa 15:12
h 1Sa 14:50
1Sa 17:55
2Sa 2:8
2Sa 3:8
i 1Sa 26:8
j 1Sa 14:45
k 2Sa 12:5
2Sa 19:28
l 1Sa 14:16
m 1Sa 9:16
1Sa 10:1
n 1Sa 26:11
1Fa 19:6

Daudi mwanangu?”[a] Naye Daudi akasema: “Ni sauti yangu, bwana wangu mfalme.”
18 Naye akaongeza kusema: “Kwa nini bwana wangu anamfuatilia mtumishi wake,[b] kwani nimefanya nini, na kuna ubaya gani mkononi mwangu?[c]
19 Na sasa, tafadhali, bwana wangu mfalme na ayasikilize maneno ya mtumishi wake: Ikiwa ni Yehova aliyekuchochea juu yangu, na anuse harufu ya toleo la nafaka.[d] Lakini ikiwa ni wanadamu,[e] wamelaaniwa mbele za Yehova,[f] kwa sababu leo wamenifukuza nisione kuwa nimeshikamana na urithi wa Yehova,[g] wakisema, ‘Nenda, tumikia miungu mingine!’[h] **20** Na sasa usiache damu yangu imwagike chini mbele za uso wa Yehova;[i] kwa maana mfalme wa Israeli ametoka kwenda kutafuta kiroboto mmoja,[j] kama vile mtu anavyomfukuza kwale juu ya milima.”[k]

21 Naye Sauli akasema: “Nimetenda dhambi.[l] Rudi, Daudi mwanangu, kwa maana sitakudhuru tena, kwa sababu ya ukweli wa kwamba nafsi yangu imekuwa na thamani[m] machoni pako leo. Tazama! Nimetenda kipumbavu, nami nimekosea sana.” **22** Ndipo Daudi akajibu na kusema: “Tazama, mkuki wa mfalme ni huu, basi mmoja wa vijana na aje, auchukue. **23** Na Yehova ndiye atakayemlipa kila mmoja uadilifu[n] wake na uaminifu wake, kwa kuwa Yehova leo alikutia mkononi mwangu, nami sikutaka kunyoosha mkono wangu juu ya mtiwa-mafuta wa Yehova.[o]
24 Na tazama! kama vile nafsi yako ilivyokuwa yenye thamani machoni pangu leo hii, vivyo hivyo nafsi yangu na iwe yenye thamani machoni pa Yehova,[a] ili anikomboe kutoka katika taabu yote.”[b] **25** Ndipo Sauli akamwambia Daudi: “Ubarikiwe, Daudi mwanangu. Bila shaka utafanya kazi nawe bila shaka utakuwa mshindi.”[c] Daudi akaenda zake; lakini Sauli akarudi kwake.[d]

27 Hata hivyo, Daudi akasema moyoni mwake: “Sasa mkono wa Sauli utanifagilia mbali siku moja. Hakuna jambo bora kwangu kuliko kuponyoka[e] bila shaka, niende katika nchi ya Wafilisti;[f] na Sauli atakata tamaa ya kunitafuta tena katika eneo lote la Israeli,[g] nami nitaponyoka kutoka mkononi mwake.”
2 Basi Daudi akaondoka, yeye pamoja na watu mia sita[h] waliokuwa pamoja naye, akavuka kwenda kwa Akishi[i] mwana wa Maoki, mfalme wa Gathi. **3** Na Daudi akaendelea kukaa na Akishi katika Gathi, yeye pamoja na watu wake, kila mmoja na nyumba yake,[j] Daudi na wake zake wawili, Ahinoamu[k] Myezreeli na Abigaili,[l] mke wa Nabali Mkarmeli. **4** Baada ya muda Sauli akapelekewa habari kwamba Daudi alikuwa amekimbia kwenda Gathi, kwa hiyo hakwenda kumtafuta tena.[m]

5 Ndipo Daudi akamwambia Akishi: “Ikiwa sasa nimepata kibali machoni pako, na wanipe mahali katika moja la majiji ya mashambani, ili nikae huko; kwa nini mtumishi wako akae katika jiji la kifalme pamoja nawe?” **6** Basi Akishi akampa Siklagi[n] siku hiyo. Ndiyo sababu Siklagi limekuwa la wafalme wa Yuda mpaka leo hii.

7 Na hesabu ya siku ambazo Daudi alikaa katika nchi ya mashambani ya Wafilisti ika-

SURA 26

a 1Sa 24:8
1Sa 24:16
b Zb 35:7
Zb 69:4
c 1Sa 24:9
1Sa 24:11
Zb 7:3
Yoh 10:32
Yoh 18:23
d Law 19:5
2Sa 24:25
e 1Sa 24:9
f Met 30:10
g Kut 19:5
Kum 26:18
Kum 32:9
2Sa 20:19
Zb 135:4
h Ro 14:13
i Yak 5:6
j 1Sa 24:14
k Omb 3:52
l Kut 9:27
1Sa 15:24
1Sa 24:17
Mt 27:4
m 1Sa 24:10
1Sa 26:11
n 1Fa 8:32
Zb 7:8
Zb 18:20
Zb 28:4
o 1Sa 24:6
1Sa 26:9

Safu ya 2

a Zb 18:25
Mt 5:7
Mt 7:2
b Mwa 48:16
Zb 34:19
2Pe 2:9
c 1Sa 24:19
Isa 54:17
d Mwa 18:33
Hes 24:25
1Sa 24:22
1Sa 27:4
2Sa 19:39

SURA 27

e 1Sa 19:18
1Sa 22:1
1Sa 22:5
f 1Sa 28:1
1Sa 29:2
g 1Sa 18:29
1Sa 23:23
h 1Sa 25:13
1Sa 30:9
i 1Sa 21:10
1Sa 27:12
j 1Ti 5:8
k 1Sa 25:43
l 1Sa 25:39
1Sa 25:42
m 1Sa 23:14
1Sa 26:25
n Yos 19:5
1Sa 30:1
2Sa 1:1
1Nya 4:30
1Nya 12:1
1Nya 12:20
Ne 11:28

wa mwaka mmoja na miezi minne.[a] **8** Na Daudi akapanda pamoja na watu wake ili wavamie Wageshuri[b] na Wagirzi na Waamaleki;[c] kwa maana walikuwa wakikaa katika nchi iliyoanzia Telamu[d] mpaka Shuri[e] na kushuka mpaka nchi ya Misri. **9** Naye Daudi akaipiga nchi, lakini hakuhifadhi hai mwanamume wala mwanamke;[f] naye akachukua makundi na mifugo na punda na ngamia na mavazi, kisha akarudi, akaja kwa Akishi. **10** Ndipo Akishi akasema: "Mlivamia wapi leo?" Naye Daudi akasema:[g] "Upande wa kusini wa Yuda[h] na upande wa kusini wa Wayerahmeeli[i] na upande wa kusini wa Wakeni."[j] **11** Na kuhusu mwanamume na mwanamke, Daudi hakuhifadhi hai yeyote ili kuwaleta Gathi, akisema: "Wasije wakatusema kwa maneno haya, 'Hivi ndivyo Daudi alivyofanya.'"[k] (Na hii imekuwa kawaida yake siku zote ambazo aliishi katika nchi ya mashambani ya Wafilisti.) **12** Kwa hiyo Akishi akamwamini[l] Daudi, akisema moyoni mwake: "Bila shaka amenuka katikati ya watu wake Israeli;[m] naye atakuwa mtumishi wangu mpaka wakati usio na kipimo."

28 Na ikawa katika siku hizo kwamba Wafilisti wakaanza kukusanya kambi zao kwa ajili ya jeshi ili kufanya vita juu ya Israeli.[n] Basi Akishi akamwambia Daudi: "Bila shaka unajua kwamba unapaswa kwenda pamoja nami kambini, wewe na watu wako."[o] **2** Kwa hiyo Daudi akamwambia Akishi: "Ndiyo sababu wewe mwenyewe unajua lile ambalo mtumishi wako anapaswa kufanya." Basi Akishi akamwambia Daudi: "Ndiyo sababu nitakuweka kuwa mlinzi wa kichwa changu sikuzote."[a]

3 Basi Samweli alikuwa amekufa, na Israeli wote walikuwa wamemwombolezea, wakamzika katika Rama jiji lake.[b] Naye Sauli alikuwa amewaondolea mbali kutoka katika nchi wenye kuwasiliana na pepo na wajuzi wa kubashiri matukio.[c]

4 Na Wafilisti wakakusanyika, wakaja na kupiga kambi katika Shunemu.[d] Kwa hiyo Sauli akakusanya pamoja Israeli wote nao wakapiga kambi katika Gilboa.[e] **5** Sauli alipoona kambi ya Wafilisti, akaogopa, na moyo wake ukaanza kutetemeka sana.[f] **6** Ingawa Sauli alikuwa akimuuliza Yehova,[g] lakini Yehova hakumjibu kamwe,[h] ama kwa ndoto[i] ama kwa Urimu[j] ama kwa manabii.[k] **7** Mwishowe Sauli akawaambia watumishi wake: "Nitafutieni mwanamke ambaye ni stadi wa kuwasiliana na pepo,[l] nami nitaenda kwake nitafute shauri kutoka kwake." Ndipo watumishi wake wakamwambia: "Tazama! Kuna mwanamke katika En-dori ambaye ni stadi wa kuwasiliana na pepo."[m]

8 Kwa hiyo Sauli akajibadili sura[n] na kuvaa mavazi mengine, akaenda, yeye na watu wawili pamoja naye; nao wakafika kwa yule mwanamke usiku.[o] Sasa akasema: "Tafadhali, nifanyie uaguzi[p] kwa kuwasiliana na pepo, unipandishie yule nitakayemtaja kwako." **9** Hata hivyo, yule mwanamke akamwambia: "Tazama, wewe mwenyewe unajua vema yale ambayo Sauli alifanya, jinsi alivyowakatilia mbali kutoka katika nchi wenye kuwasiliana na pepo na wajuzi wa kubashiri matukio.[q] Kwa nini, basi,

SURA 27

a 1Sa 29:3
b Yos 13:2
c Mwa 36:12
Kut 17:8
Kut 17:14
Hes 13:29
1Sa 15:2
2Sa 1:1
1Nya 4:43
d 1Sa 15:4
e Mwa 25:18
Kut 15:22
f Kum 25:19
1Sa 15:3
g Mt 10:16
h Yos 15:2
i 1Nya 2:9
j Hes 24:21
1Sa 15:6
k Met 22:3
l Met 14:15
m Mwa 34:30
1Sa 13:4

SURA 28

n Amu 3:2
1Sa 14:52
o 1Sa 27:12
1Sa 29:3

Safu ya 2

a 1Sa 29:2
b 1Sa 25:1
Isa 57:1
c Kut 22:18
Law 19:31
Law 20:6
Law 20:27
Kum 18:11
Ufu 21:8
d Yos 19:18
1Fa 1:3
2Fa 4:8
Wim 6:13
e 1Sa 31:1
2Sa 1:21
2Sa 21:12
f Kum 28:20
1Sa 28:20
Met 10:24
Isa 57:21
g 1Sa 14:37
1Nya 10:14
h Met 1:28
Met 28:9
Isa 1:15
Eze 20:3
Mik 3:4
i Hes 12:6
Mt 1:20
j Kut 28:30
Hes 27:21
Kum 33:8
k Zb 74:9
Omb 2:9
l Kut 22:18
Law 19:31
Law 20:6
1Sa 15:23
1Sa 28:3
Isa 8:19
Ebr 3:12
m Yos 17:11
Zb 83:10
n 1Fa 14:2
1Fa 22:30
o 1Sa 28:25
p Kum 18:10
1Nya 10:13
Isa 8:19
q 1Sa 28:3

unatenda kama mtu anayeitegea nafsi yangu mtego ili ufanye niuawe?"[a] **10** Mara moja
Sauli akamwapia kwa Yehova,
akisema: "Kama Yehova anavyoishi,[b] hutapata hatia ya kosa
katika jambo hili!" **11** Ndipo
yule mwanamke akasema: "Nikupandishie nani?" Naye akasema: "Nipandishie Samweli."[c]
12 Wakati yule mwanamke alipomwona "Samweli,"[d] akaanza
kupiga kelele kwa sauti yake
yote; na mwanamke huyo akamwambia Sauli: "Kwa nini
umenidanganya, kwa kuwa
wewe mwenyewe ndiye Sauli?" **13** Lakini mfalme akamwambia: "Usiogope, lakini uliona nini?" Mwanamke huyo
akaendelea kumwambia Sauli: "Niliona mungu[e] akipanda
juu kutoka katika dunia."
14 Mara moja akamuuliza huyo
mwanamke: "Ana umbo gani?"
naye akasema: "Ni mwanamume mzee anayepanda juu, naye
amevaa koti lisilo na mikono."[f]
Ndipo Sauli akatambua kwamba huyo alikuwa ni "Samweli,"[g] naye akainama kifudifudi,
akasujudu.

15 Naye "Samweli" akaanza
kumwambia Sauli: "Kwa nini
umenisumbua kwa kufanya nipandishwe?"[h] Na Sauli akasema: "Niko katika dhiki kali
sana,[i] kwa kuwa Wafilisti wanapigana nami, na Mungu ameniacha[j] wala hakunipa jibu tena,
ama kwa manabii ama kwa ndoto;[k] ndiyo sababu ninakuita uni-
julishe jambo nitakalofanya."[l]

16 Na "Samweli" akaendelea kusema: "Kwa nini, basi,
unaniuliza mimi, wakati ambapo Yehova mwenyewe amekuacha[m] na kwamba yeye ni adui
yako?[n] **17** Na Yehova atajifanyia kama vile alivyosema kupitia mimi, na Yehova ataurarua
ufalme kutoka mkononi mwako,[a] na kumpa mwenzako Daudi.[b] **18** Kwa vile hukusikiliza
sauti ya Yehova,[c] nawe hukutekeleza hasira yake inayowaka juu ya Amaleki,[d] ndiyo saba-
bu hakika Yehova atakutendea
jambo hili leo. **19** Na Yehova atatia Israeli pia pamoja na
wewe mkononi mwa Wafilisti,[e]
na kesho[f] wewe na wana wako[g]
mtakuwa pamoja nami. Hata
kambi ya Israeli, Yehova ataitia
mkononi mwa Wafilisti."[h]

20 Ndipo Sauli akaanguka chini upesi akiwa amejilaza chini mwili mzima, akaogopa sana kwa sababu ya maneno ya "Samweli." Pia, kukawa hakuna nguvu zozote ndani
yake, kwa sababu alikuwa hajala chakula mchana mzima
na usiku mzima. **21** Sasa yule
mwanamke akamjia Sauli, akaona kwamba alikuwa na wasiwasi sana. Kwa hiyo akamwambia: "Tazama, mjakazi wako
ameitii sauti yako, nami nikaitia nafsi yangu mkononi mwangu[i] na kuyatii maneno uliyoniambia. **22** Na sasa, tafadha-
li, wewe pia uitii sauti ya mjakazi wako; na acha niweke mbele
yako kipande cha mkate, nawe
ule, ili upate nguvu, kwa sababu utaenda zako." **23** Lakini akakataa na kusema: "Sitakula." Hata hivyo, watumishi
wake na pia yule mwanamke
wakazidi kumsihi. Mwishowe
akaitii sauti yao, akainuka kutoka chini na kuketi juu ya kiti.
24 Basi yule mwanamke alikuwa na ndama aliyenoneshwa[j]
nyumbani. Kwa hiyo akamchinja haraka,[k] akachukua unga,
akaukanda na kuoka keki zisizo
na chachu. **25** Kisha akampakulia Sauli na watumishi wake,

SURA 28
a Kut 22:18
Law 20:27
b 1Sa 14:39
Isa 48:1
Yer 44:26
c Ro 1:28
d 1Sa 28:3
Zb 146:4
Mhu 9:5
2Ko 4:4
2Ko 11:14
e Zb 82:6
Yoh 10:34
f 1Sa 15:27
g 2Th 2:10
2Th 2:11
h 2Sa 12:23
Zb 115:17
Zb 146:4
Mhu 9:5
Mhu 9:10
i Met 14:14
Yer 2:17
Ga 6:7
j 1Sa 15:23
k 1Sa 28:6
l Law 19:31
m 1Sa 15:23
1Sa 16:14
2Fa 6:27
n Kum 28:15

Safu ya 2
a 1Sa 13:14
1Sa 15:28
b 1Sa 16:13
1Sa 24:20
c 1Sa 13:11
1Nya 10:13
d 1Sa 15:9
Yer 48:10
e 1Sa 12:25
1Sa 28:1
1Sa 31:1
f 1Sa 31:5
g 1Sa 31:2
2Sa 2:8
h 1Sa 31:7
i Law 20:27
Amu 12:3
1Sa 19:5
Ayu 13:14
j Mwa 18:7
Lu 15:23
k Kum 12:15

nao wakala. Ndipo wakaondoka, wakaenda zao usiku huo.[a]

29 Na Wafilisti[b] wakakusanya kambi zao zote kule
Afeki, huku Waisraeli wakipiga kambi kando ya bubujiko lililo katika Yezreeli.[c] **2** Na wakuu wa muungano wa Wafilisti[d] walikuwa wakipita kwa mamia na kwa maelfu, na Daudi
na watu wake walikuwa wakipita baadaye pamoja na Akishi.[e]
3 Nao wakuu wa Wafilisti wakaanza kusema: "Hawa Waebrania[f] wanataka nini?" Naye
Akishi akawaambia wakuu wa Wafilisti: "Je, huyu si Daudi mtumishi wa Sauli mfalme wa Israeli, aliyekuwa pamoja nami hapa mwaka mmoja au miwili,[g] nami sijapata[h]ndani yake jambo hata moja tangu siku ile alipotoroka kuja kwangu mpaka leo hii?" **4** Nao wakuu wa Wafilisti wakamghadhibikia; na wakuu Wafilisti wakaendelea kumwambia: "Mrudishe mtu huyo,[i] mwache arudi mahali ulipompa; wala usiache ashuke pamoja nasi kwenda vitani, asije akawa mpinzani[j] wetu katika vita. Na je, mtu huyu atajipatia kibali kwa bwana wake jinsi gani? Je, si kwa vichwa vya watu wetu? **5** Je, huyu si Daudi ambaye waliendelea kuitikia katika kucheza dansi, wakisema, 'Sauli amepiga maelfu yake, na Daudi makumi ya maelfu yake'?"[k]

6 Basi Akishi[l] akamwita Daudi na kumwambia: "Kama Yehova anavyoishi,[m] wewe ni mnyoofu, na kutoka kwako na kuingia kwako[n] pamoja nami katika kambi kumekuwa kwema machoni pangu;[o] kwa maana sijapata ubaya ndani yako tangu siku ile ulipokuja kwangu mpaka leo hii.[p] Lakini machoni pa wakuu wa muungano[a] wewe si mwema. **7** Na sasa rudi, uende kwa amani, usije ukafanya jambo lolote baya machoni pa wakuu wa muungano wa Wafilisti." **8** Hata hivyo, Daudi akamwambia Akishi: "Kwani nimefanya nini,[b] nawe umepata nini ndani ya mtumishi wako tangu siku ile nilipokuja mbele yako mpaka leo hii,[c] ili nisije na kupigana na adui za bwana wangu mfalme?" **9** Ndipo Akishi akajibu na kumwambia Daudi: "Najua vema kwamba umekuwa mwema machoni pangu, kama malaika wa Mungu.[d] Ila wakuu wa Wafilisti ndio wamesema, 'Asipande pamoja nasi kwenda vitani.' **10** Na sasa ondokeni asubuhi na mapema pamoja na watumishi wa bwana wako waliokuja nawe; nanyi mwondoke asubuhi na mapema wakati kutakapokuwa kumewapambazukia. Kisha mwende zenu."[e]

11 Basi Daudi akaondoka mapema, yeye na watu wake, ili waende asubuhi[f] na kurudi katika nchi ya Wafilisti; nao Wafilisti wakapanda, wakaenda Yezreeli.[g]

30 Na ikawa kwamba, wakati Daudi na watu wake walipokuwa wakija Siklagi[h] siku ya tatu, Waamaleki[i] wakavamia upande wa kusini na pia Siklagi; wakapiga Siklagi, wakaliteketeza kwa moto, **2** nao wakachukua mateka wanawake[j] na vyote vilivyokuwa ndani yake, kuanzia mdogo zaidi mpaka mkubwa zaidi. Hawakumuua yeyote, bali waliwachukua na kwenda zao. **3** Daudi alipokuja jijini na watu wake, tazama, jiji lilikuwa limeteketezwa kwa moto, na wake zao na wana wao na binti zao

SURA 28
a 1Sa 28:8

SURA 29
b 1Sa 28:1
c Yos 19:18
1Sa 29:11
2Sa 4:4
d Yos 13:3
Amu 3:3
1Sa 5:8
e 1Sa 28:2
f 1Sa 13:19
2Ko 11:22
g 1Sa 27:7
h 1Sa 27:12
Met 14:15
i 1Nya 12:19
j 1Sa 14:21
k 1Sa 18:7
1Sa 21:11
l 1Sa 21:10
1Sa 27:2
m 1Sa 20:21
Yer 12:16
n Hes 27:17
Zb 121:8
o 1Sa 28:2
p 1Sa 27:11
1Sa 27:12
1Sa 29:3
Mt 10:16

Safu ya 2
a 1Sa 29:2
b 1Sa 27:11
c 1Sa 28:2
d 1Sa 27:12
2Sa 14:17
2Sa 14:20
2Sa 19:27
Met 14:35
Ga 4:14
e Zb 37:23
Met 16:9
Met 21:1
Yer 10:23
2Pe 2:9
f Zb 91:11
Zb 119:133
g Yos 19:18
1Sa 29:1
2Sa 4:4

SURA 30
h Yos 15:31
1Sa 27:6
i Mwa 36:12
Kut 17:14
1Sa 15:2
1Sa 27:8
j Amu 5:30
1Sa 27:3

walikuwa wamechukuliwa mateka. **4** Na Daudi na watu waliokuwa pamoja naye wakaanza
kupaaza sauti zao, wakalia,[a]
mpaka nguvu za kuendelea kulia zilipokwisha ndani yao.
5 Na wake wawili wa Daudi
walikuwa wamechukuliwa mateka, Ahinoamu[b] Myezreeli, na
Abigaili[c] mke wa Nabali Mkarmeli. **6** Naye Daudi akataabika sana,[d] kwa sababu watu walisema apigwe kwa mawe;[e] kwa
maana nafsi za watu wote zilikuwa zimeingiwa na uchungu;[f]
kila mmoja kwa sababu ya wanawe na binti zake. Basi Daudi
akajitia nguvu kwa Yehova Mungu wake.[g]

7 Hivyo Daudi akamwambia
Abiathari[h] kuhani, mwana wa
Ahimeleki: "Tafadhali ilete hapa
efodi."[i] Naye Abiathari akamletea Daudi ile efodi. **8** Daudi
akaanza kumuuliza Yehova,[j] akisema: "Je, nikifuatilie kikundi hiki cha waporaji? Je, nitawafikia?"[k] Ndipo akamwambia:
"Nenda, uwafuatilie, kwa maana bila shaka utawafikia, nawe
bila shaka utaleta ukombozi."[l]

9 Mara moja Daudi akaondoka, yeye pamoja na wale watu
mia sita[m] waliokuwa naye, wakaenda mpaka bonde la mto
la Besori, na watu ambao walipaswa kuachwa nyuma wakasimama tuli. **10** Na Daudi akaendelea kufuatilia,[n] yeye pamoja na watu mia nne, lakini watu
mia mbili waliokuwa wamechoka sana wasiweze kuvuka lile
bonde la mto la Besori[o] wakasimama tuli.

11 Nao wakakuta mtu, Mmisri,[p] shambani. Basi wakampeleka kwa Daudi na kumpa mkate ale, na kumpa maji anywe.
12 Zaidi ya hayo, wakampa
kipande cha keki ya tini zilizoshinikizwa na keki mbili za
zabibu kavu.[a] Ndipo akala
na roho[b] yake ikarudi kwake;
kwa maana hakuwa amekula mkate wala kunywa maji kwa
siku tatu, mchana na usiku.
13 Sasa Daudi akamwambia:
"Wewe ni wa nani, nawe unatoka wapi?" naye akasema: "Mimi
ni mtumishi Mmisri, mtumwa
wa mtu Mwamaleki, lakini bwana wangu aliniacha kwa sababu nilishikwa na ugonjwa siku
tatu zilizopita.[c] **14** Sisi ndio
tuliovamia upande wa kusini
wa Wakerethi[d] na nchi ya Yuda
na upande wa kusini wa Kalebu;[e] nasi tukateketeza Siklagi kwa moto." **15** Naye Daudi
akamwambia: "Je, utaniongoza, nishuke mpaka kwenye hiki
kikundi cha waporaji?" Naye
akasema: "Niapie[f] kwa Mungu
kwamba hutaniua, wala kunitia mkononi mwa bwana wangu,[g] nami nitakuongoza, ushuke mpaka kwenye hiki kikundi
cha waporaji."

16 Basi akamwongoza, akashuka,[h] na tazama, walikuwa
wameenea bila utaratibu juu ya
uso wote wa nchi, wakila na kunywa na kufanya karamu[i] kwa
sababu ya nyara yote kubwa
ambayo walikuwa wamechukua
kutoka katika nchi ya Wafilisti
na nchi ya Yuda.[j] **17** Na Daudi akawapiga kuanzia giza la
asubuhi mpaka jioni, apate kuwaangamiza; wala hakuna mtu
kati yao aliyeponyoka[k] ila vijana mia nne waliopanda ngamia
na kukimbia. **18** Naye Daudi
akakomboa vyote ambavyo Waamaleki walikuwa wamechukua,[l]
na Daudi akakomboa
wake zake wawili. **19** Na hakuna kitu chochote chao kilichokosekana, kuanzia mdogo
zaidi mpaka mkubwa zaidi na

SURA 30

a Amu 21:2
b 1Sa 25:43
2Sa 2:2
c 1Sa 25:42
1Sa 27:3
d Zb 25:17
Zb 116:3
e Kut 17:4
Hes 14:10
f Amu 18:25
1Sa 22:2
2Sa 17:8
2Fa 4:27
g Zb 18:6
Zb 27:1
Zb 31:1
Zb 31:9
Zb 34:19
Zb 43:5
Zb 56:4
Zb 143:5
Met 18:10
Hab 3:18
Lu 22:43
h 1Sa 22:20
1Fa 2:26
i 1Sa 23:9
j Hes 27:21
Amu 18:5
Amu 20:28
1Sa 23:2
1Sa 23:11
1Sa 28:6
Met 3:5
k 1Sa 14:37
Zb 28:6
l 1Sa 30:18
Zb 34:19
Met 11:8
Met 24:16
m 1Sa 23:13
1Sa 27:2
n Amu 8:4
o 1Sa 30:21
p Kum 23:7

Safu ya 2

a 1Sa 25:18
b Amu 15:19
c Met 12:10
d 2Sa 8:18
1Fa 1:38
1Nya 18:17
Eze 25:16
Sef 2:5
e Yos 14:13
Yos 21:12
f Kum 6:13
Yos 2:12
Yos 9:15
g Kum 23:15
Kum 23:16
h Amu 1:25
i Da 5:1
Lu 12:19
j Yos 15:1
Ayu 20:5
k Kut 17:14
Zb 73:19
l 1Sa 30:3

wana na mabinti na kuanzia
nyara, mpaka chochote amba-
cho walikuwa wamejichuku-
lia.[a] Daudi alirudisha kila kitu.
20 Basi Daudi akachukua ma-
kundi yote na mifugo, ambayo
waliitanguliza mbele ya ile mi-
fugo mingine. Kisha wakasema:
"Hii ni nyara ya Daudi."[b]
21 Mwishowe Daudi akawa-
fikia wale wanaume mia mbili[c]
ambao walikuwa wamechoka
sana wasiweze kwenda na Dau-
di, na ambao waliwaacha wake-
ti kando ya bonde la mto la
Besori; nao wakatoka kuja kum-
pokea Daudi na kuwapokea
watu waliokuwa pamoja naye.
Daudi alipowakaribia watu hao,
akaanza kuwauliza hali yao.
22 Hata hivyo, kila mtu mba-
ya na asiyefaa kitu[d] kati ya
watu walioenda pamoja na Da-
udi akajibu na kuzidi kusema:
"Kwa kuwa hawakwenda pamo-
ja nasi, hatutawapa nyara yoyo-
te ambayo tumekomboa, isipo-
kuwa kila mmoja atapewa mke
wake na wanawe, wawachukue
na kwenda." **23** Lakini Daudi
akasema: "Ndugu zangu, msifa-
nye hivyo na vitu ambavyo Ye-
hova ametupa sisi,[e] kwa kuwa
alitulinda[f] na kukitia mkono-
ni mwetu kile kikundi cha wa-
poraji kilichokuja juu yetu.[g]
24 Na ni nani atakayewasikiliza
kwa neno hili? Kwa maana
kama lilivyo fungu la yule ali-
yeshuka kwenda vitani ndi-
vyo litakavyokuwa fungu la
yule aliyeketi kando ya mizigo.[h]
Wote watapata fungu pamoja."[i]
25 Na ikawa kwamba kuanzia
siku hiyo na kuendelea, akali-
weka hilo kuwa sharti na uamu-
zi wa hukumu[j] kwa ajili ya Isra-
eli mpaka leo hii.
26 Wakati Daudi alipofika Sik-
lagi, akapeleka sehemu ya nyara
kwa wanaume wazee wa Yuda,
rafiki zake,[a] akisema: "Tazame-
ni, hii ni zawadi[b] ya bara-
ka kwa ajili yenu kutoka ka-
tika nyara za adui za Yehova."
27 Kwa wale waliokuwa Be-
theli,[c] na kwa wale waliokuwa
Ramothi[d] la kusini, na kwa
wale waliokuwa Yatiri,[e] **28** na
kwa wale waliokuwa Aroeri, na
kwa wale waliokuwa Sifmothi,
na kwa wale waliokuwa Eshte-
moa,[f] **29** na kwa wale waliokuwa
Rakali, na kwa wale waliokuwa
katika majiji ya Wayerahmeeli,[g]
na kwa wale waliokuwa katika
majiji ya Wakeni,[h] **30** na
kwa wale waliokuwa Horma,[i] na
kwa wale waliokuwa Borashani,[j]
na kwa wale waliokuwa Atha-
ki, **31** na kwa wale waliokuwa
Hebroni,[k] na mahali pote amba-
po Daudi alikuwa ametembea,
yeye pamoja na watu wake.

31 Basi Wafilisti walikuwa
wakipigana na Israeli,[l] na
watu wa Israeli wakaanza ku-
kimbia kutoka mbele ya Wafi-
listi, nao wakaendelea kuangu-
ka, wakiwa wameuawa[m] kati-
ka Mlima Gilboa.[n] **2** Na Wa-
filisti wakaendelea kumfuatilia
kwa ukaribu sana Sauli na wa-
nawe; na mwishowe Wafilisti
wakawapiga na kuwaua Yona-
thani[o] na Abinadabu[p] na Malki-
shua,[q] wana wa Sauli. **3** Na pi-
gano likawa kali juu ya Sauli, na
mwishowe wapiga-mishale, wa-
piga-upinde, wakampata, na
hao wapiga-mishale wakamu-
umiza vibaya.[r] **4** Ndipo Sau-
li akamwambia mchukua-silaha
wake: "Chomoa upanga wako,[s]
unichome nao, ili watu hawa
wasiotahiriwa[t] wasije na kuni-
choma na kunitendea vibaya."
Naye mchukua-silaha wake ha-
kutaka,[u] kwa sababu aliogo-
pa sana. Basi Sauli akachukua

SURA 30
a 1Sa 30:8
Zb 34:19
b Hes 31:9
2Nya 20:25
c 1Sa 30:10
d 1Sa 10:27
Nah 1:15
e 1Nya 29:12
Zb 33:16
f Hes 31:49
g 1Sa 30:8
Zb 44:3
h 1Sa 10:22
1Sa 17:22
1Sa 25:13
1Sa 30:10
i Hes 31:27
Yos 22:8
Zb 68:12
1Ti 6:18
j Hes 27:11

Safu ya 2
a Isa 32:8
b Mwa 33:11
2Fa 5:15
Met 11:24
Met 18:16
Mdo 20:35
c Yos 19:4
d Yos 19:8
e Yos 15:48
Yos 21:14
f Yos 15:50
Yos 21:14
g 1Sa 27:10
1Nya 2:9
1Nya 2:26
h Amu 1:16
1Sa 15:6
i Yos 19:4
Amu 1:17
j Yos 19:7
k Yos 14:13
2Sa 2:1

SURA 31
l 1Sa 14:52
1Sa 29:1
m 1Sa 12:25
1Nya 10:1
n 1Sa 28:4
2Sa 1:21
o 1Sa 13:2
p 1Nya 8:33
q 1Nya 9:39
r 2Sa 1:4
2Sa 1:6
s Amu 9:54
1Nya 10:4
t 1Sa 14:6
1Sa 17:26
2Sa 1:20
Eze 44:7
u 1Sa 22:17
2Sa 1:14
Zb 105:15

upanga, akauangukia.[a] **5** Wakati yule mchukua-silaha wake
alipoona kwamba Sauli amekufa,[b] ndipo yeye pia akauangukia
upanga wake mwenyewe, akafa
pamoja naye.[c] **6** Basi Sauli na
wanawe watatu na mchukua-silaha wake, watu wake wote, wa-
kafa pamoja siku hiyo.[d] **7** Wa-
kati watu wa Israeli waliokuwa katika eneo la nchi tambarare ya chini na waliokuwa katika
eneo la Yordani walipoona kwa-
mba watu wa Israeli wamekimbia, na kwamba Sauli na wana-
we wamekufa, ndipo wakaanza
kuyaacha majiji na kukimbia,[e]
kisha Wafilisti wakaingia na ku-
anza kukaa ndani yake.[f]

8 Na kesho yake ikawa kwa-
mba, Wafilisti walipokuja ku-
wavua waliouawa,[g] wakamkuta
Sauli na wanawe watatu wame-
anguka juu ya Mlima Gilboa.[h]
9 Nao wakakata kichwa[i] chake na kuvua silaha zake na ku-
tuma wajumbe kotekote katika nchi ya Wafilisti ili kuzijulisha[a] nyumba za sanamu[b] zao
pamoja na watu. **10** Mwisho-
we wakaweka silaha[c] zake katika nyumba za sanamu za Ashto-
rethi,[d] nao wakafunga maiti
yake kwenye ukuta wa Beth-
shani.[e] **11** Na kumhusu yeye,
wakaaji wa Yabesh-gileadi[f] wa-
kasikia yale ambayo Wafilisti
walikuwa wamemtendea Sauli.
12 Mara moja wanaume wote
mashujaa wakaondoka, waka-
enda usiku kucha, wakachu-
kua maiti ya Sauli na maiti
za wanawe kutoka katika uku-
ta wa Beth-shani, wakaja mpa-
ka Yabeshi na kuziteketeza kwa
moto hapo.[g] **13** Kisha waka-
chukua mifupa yao,[h] na kuizi-
ka[i] chini ya mkwaju[j] ulio kati-
ka Yabeshi, nao wakafunga kwa
siku saba.[k]

SURA 31
a Kut 20:13
2Sa 17:23
1Fa 16:18
1Nya 10:4
Mt 27:5
b 1Sa 26:10
1Nya 10:13
Ho 13:11
c 1Nya 10:5
d 1Sa 28:19
1Nya 10:6
e Kum 28:25
1Sa 13:6
f Hes 33:56
Kum 28:33
1Nya 10:7
g 1Nya 10:8
2Nya 20:25
h 1Sa 28:4
1Sa 31:1
2Sa 1:6
2Sa 21:12
i 1Sa 17:51
1Nya 10:9

Safu ya 2
a 2Sa 1:20
b Amu 16:23
c 1Sa 21:9
1Nya 10:10
d Amu 2:13
e Yos 17:11
Amu 1:27
2Sa 21:12
f 1Sa 11:1
2Sa 2:4
2Sa 21:12
1Nya 10:11
g Amo 6:10
h 2Sa 21:12
i Mwa 35:8; 2Sa 2:5; j Mwa 21:33; 1Sa 22:6; 1Nya 10:12; k Mwa 50:10.

KITABU CHA PILI CHA

SAMWELI

au, kulingana na *Septuajinti* ya Kigiriki,
KITABU CHA PILI CHA WAFALME

1 Na ikawa baada ya kifo cha
Sauli, na wakati Daudi ali-
pokuwa amerudi kutoka kuwa-
piga Waamaleki,[a] kwamba Dau-
di akaendelea kukaa siku mbi-
li katika Siklagi.[b] **2** Na ika-
wa kwamba katika siku ya
tatu, tazama! mtu[c] fulani aliku-
wa anakuja kutoka katika ka-
mbi, kutoka kwa Sauli, mava-
zi yake yakiwa yameraruliwa[d]
na mavumbi yakiwa juu ya ki-
chwa chake;[e] na ikawa alipo-
mjia Daudi, akaanguka chini[f]
mara moja na kulala kifudi-
fudi.

3 Naye Daudi akamwambia:
"Umetoka wapi?" naye akamji-
bu: "Nimekimbia kutoka ka-
tika kambi ya Israeli." **4** Na
Daudi akaendelea kumwambia:
"Mambo yaliendaje? Niambie ta-
fadhali." Naye akasema: "Watu
wamekimbia kutoka vitani na
pia watu wengi wameanguka,
wakafa,[a] na hata Sauli[b] na Yo-
nathani[c] mwana wake wameku-
fa pia." **5** Kisha Daudi akamu-

SURA 1
a 1Sa 30:17
b 1Sa 27:6
1Sa 30:26
c 2Sa 4:10
d Mwa 37:29
Hes 14:6
Yos 7:6
e 1Sa 4:12
f 1Sa 25:23
2Sa 14:4

Safu ya 2
a 1Sa 31:1
b 1Sa 31:6
1Nya 10:4
c 1Sa 31:2
1Nya 10:6

uliza yule kijana aliyekuwa akimpasha habari: "Unajuaje hakika kwamba Sauli amekufa, na pia Yonathani mwana wake?"[a]
6 Ndipo yule kijana aliyekuwa akimpasha habari akasema: "Nilijikuta katika Mlima Gilboa[b] bila kutazamia, na tazama, Sauli alikuwa amejiegemeza kwenye mkuki wake;[c] na tazama! waendesha-magari na wapandafarasi walikuwa wamemfikia.[d]
7 Alipogeuka nyuma na kuniona, akaniita, nami nikasema, 'Mimi hapa!' **8** Naye akaendelea kuniambia, 'Wewe ni nani?' nami nikamwambia, 'Mimi ni Mwamaleki.'[e] **9** Kisha akasema, 'Tafadhali, simama juu yangu, na kwa hakika uniue, kwa maana ganzi imenishika, kwa sababu nafsi[f] yangu yote ingali ndani yangu.' **10** Basi nikasimama juu yake na kwa hakika nikamuua,[g] kwa maana nilijua kwamba hangeishi baada ya kuanguka. Kisha nikachukua taji[h] lililokuwa juu ya kichwa chake na kikuku kilichokuwa kwenye mkono wake, ili nivilete kwa bwana wangu hapa."

11 Ndipo Daudi akashika mavazi yake akayararua,[i] na pia watu wote waliokuwa pamoja naye wakafanya hivyo.
12 Nao wakaanza kuomboleza na kulia[j] na kufunga[k] mpaka jioni kwa ajili ya Sauli na kwa ajili ya Yonathani mwana wake na kwa ajili ya watu wa Yehova na kwa ajili ya nyumba ya Israeli,[l] kwa sababu walikuwa wameanguka kwa upanga.

13 Basi Daudi akamwambia yule kijana aliyekuwa akimpasha habari: "Unatoka wapi wewe?" naye akajibu: "Mimi ni mwana wa mkaaji mgeni, Mwamaleki."[m]
14 Kisha Daudi akamwambia: "Kwa nini hukuogopa[n] kunyoosha mkono wako umwangamize mtiwa-mafuta[a] wa Yehova?"
15 Kwa hiyo Daudi akamwita mmoja wa vijana na kumwambia: "Sogea karibu. Mpige." Basi akampiga, naye akafa.[b] **16** Ndipo Daudi akamwambia: "Hatia yako ya damu na iwe juu ya kichwa chako mwenyewe,[c] kwa sababu kinywa chako mwenyewe kimetoa ushuhuda juu yako,[d] kusema, 'Mimi mwenyewe kwa hakika nilimuua mtiwa-mafuta wa Yehova.'"[e]

17 Na Daudi akaimba wimbo huu wa huzuni[f] kwa ajili ya Sauli na Yonathani mwana wake[g]
18 na kusema kwamba wana wa Yuda[h] wafundishwe "Upinde."[i] Tazama! Umeandikwa katika kitabu cha Yashari:[j]

19 "Ee Israeli, uzuri umeuawa
katika mahali pako
pa juu.[k]
Lo! Jinsi walivyoanguka
wanaume wenye nguvu!
20 Msiseme hayo katika Gathi;[l]
Msiyatangaze katika
barabara za Ashkeloni,[m]
Binti za Wafilisti wasije
wakashangilia,
Binti za watu
wasiotahiriwa wasije
wakafurahi.[n]
21 Enyi milima ya Gilboa,[o]
umande wowote, wala
mvua yoyote isinyeshe
juu yenu, wala kusiwe
na mashamba ya
michango mitakatifu;[p]
Kwa sababu ngao ya
wenye uwezo
ilichafuliwa hapo,
Ngao ya Sauli, hata
kukawa hakuna yoyote
iliyotiwa mafuta.[q]
22 Kutoka kwa damu ya
waliouawa, kutoka kwa
mafuta ya wenye uwezo,

SURA 1

a Met 14:15
Met 25:2
b 1Sa 28:4
1Nya 10:1
c 1Sa 18:10
1Sa 19:9
1Sa 22:6
1Sa 26:12
d 1Sa 31:3
1Nya 10:3
e Kut 17:16
Hes 24:20
Kum 25:19
1Sa 15:20
1Sa 30:1
1Sa 30:18
f Mwa 2:7
g 1Sa 31:4
Zb 5:6
Yoh 8:44
h 2Fa 11:12
i 2Sa 3:31
2Sa 13:31
2Nya 34:27
Mdo 14:14
j Kum 34:8
k 1Sa 31:13
l 1Sa 31:1
2Sa 1:4
m 2Sa 1:8
n Hes 12:8
1Sa 31:4

Safu ya 2

a 1Sa 24:6
1Sa 26:9
Zb 105:15
b 2Sa 4:10
1Fa 2:25
c Yos 2:19
Amu 9:24
2Sa 4:11
1Fa 2:37
Eze 18:13
Mdo 18:6
d Met 19:5
Met 21:28
e 2Sa 1:10
f 2Sa 3:33
2Nya 35:25
g 1Sa 31:6
h Mwa 49:8
1Sa 30:26
i 1Sa 20:36
1Sa 31:3
2Sa 1:22
j Yos 10:13
k 1Sa 31:8
Omb 2:1
l Kum 32:27
1Sa 31:9
m Yos 13:3
Amu 16:23
1Sa 6:17
n Kum 28:37
o 1Sa 31:1
1Nya 10:1
p Law 27:16
q Isa 21:5

Upinde wa Yonathani
haukugeuka nyuma,[a]
Na upanga wa
Sauli haukurudi bila
mafanikio.[b]
23 Sauli na Yonathani,[c] watu
wenye kupendwa na
wenye kupendeza wakati
wa maisha yao,
Nao hawakutenganishwa
katika kifo chao.[d]
Walikuwa wepesi kuliko
tai,[e]
Walikuwa wenye nguvu
kuliko simba.[f]
24 Enyi binti za Israeli,
mlilieni Sauli,
Aliyewavika nguo
nyekundu kwa
umaridadi,
Aliyeweka mapambo ya
dhahabu juu ya mavazi
yenu.[g]
25 Lo! Jinsi wenye nguvu
walivyoanguka katikati
ya pigano![h]
Yonathani ameuawa juu ya
mahali pako pa juu![i]
26 Nimesikitika kwa ajili yako,
Yonathani ndugu yangu,
Ulinipendeza sana.[j]
Upendo wako kwangu
ulikuwa wa ajabu sana
kuliko upendo kutoka
kwa wanawake.[k]
27 Lo! Jinsi wenye uwezo
walivyoanguka[l]
Na silaha za vita kuangamia!"

2 Na ikawa baadaye kwamba Daudi akamuuliza Yehova,[m] akisema: "Je, nipande kwenda katika moja la majiji ya Yuda?" Ndipo Yehova akamwambia: "Panda uende." Na Daudi akaendelea kusema: "Nipande kwenda wapi?" Ndipo akasema: "Hebroni."[n] 2 Basi Daudi akaenda huko na wake zake wawili pia, Ahinoamu[a] Myezreeli, na Abigaili[b] mke wa Nabali Mkarmeli. 3 Na Daudi akawaleta wale watu[c] waliokuwa pamoja naye, kila mmoja na nyumba yake; nao wakaanza kukaa katika majiji ya eneo la Hebroni. 4 Ndipo watu wa Yuda[d] wakaja, wakamtia Daudi mafuta[e] hapo awe mfalme juu ya nyumba ya Yuda.[f]

Nao wakaja kumwambia Daudi, wakisema: "Watu wa Yabesh-gileadi ndio waliomzika Sauli." 5 Basi Daudi akatuma wajumbe kwa watu wa Yabesh-gileadi[g] na kuwaambia: "Mbarikiwe na Yehova,[h] kwa kuwa mmeonyesha hizi fadhili zenye upendo[i] kwa bwana wenu, kwa Sauli, kwa maana mlimzika.[j] 6 Na sasa Yehova na awaonyeshe ninyi fadhili zenye upendo[k] na uaminifu, nami pia nitawaonyesha wema huu kwa sababu mmefanya jambo hili.[l] 7 Na sasa mikono yenu na ijitie nguvu na muwe wanaume mashujaa,[m] kwa sababu Sauli bwana wenu amekufa, na nyumba ya Yuda wamenitia mimi mafuta niwe mfalme[n] juu yao."

8 Lakini Abneri[o] mwana wa Neri mkuu wa jeshi lililokuwa la Sauli, alimchukua Ish-boshethi,[p] mwana wa Sauli, akamvusha mpaka Mahanaimu,[q] 9 akamfanya kuwa mfalme juu ya Gileadi[r] na Waashuri na Yezreeli[s] na juu ya Efraimu[t] na Benyamini[u] na juu ya Israeli yote. 10 Ish-boshethi, mwana wa Sauli, alikuwa na umri wa miaka 40 alipokuwa mfalme juu ya Israeli, naye akatawala akiwa mfalme kwa miaka miwili. Ni nyumba ya Yuda[v] peke yao ndio waliomfuata Daudi.

SURA 1
a 1Sa 18:4; 1Sa 20:20
b 1Sa 14:47
c 1Sa 18:1
d 1Sa 31:6; 1Nya 10:6
e Ayu 9:26; Yer 4:13; Omb 4:19; Hab 1:8
f Amu 14:18; Met 30:30
g Mwa 24:53
h 2Sa 1:19
i 1Sa 31:8; 2Sa 1:19
j 1Sa 18:1
k Ru 1:17; 1Sa 18:3; 1Sa 19:2; 1Sa 20:17; 1Sa 20:41; 1Sa 23:16; Met 17:17; Met 18:24
l 2Sa 1:19

SURA 2
m Hes 27:21; Amu 1:1; 1Sa 28:6; 1Sa 30:8
n Mwa 23:2; Hes 13:22; Yos 14:14; Yos 20:7; Yos 21:11; Yos 21:12; 1Sa 30:31; 2Sa 5:1; 1Fa 2:11

Safu ya 2
a 1Sa 25:43; 1Sa 30:5
b 1Sa 25:42
c 1Sa 22:2; 1Sa 27:2; 1Nya 12:1
d Mwa 49:10; 2Sa 19:11; 2Sa 19:42
e 1Sa 16:13
f 1Sa 15:28; 2Sa 5:5; 1Nya 11:3
g 1Sa 31:11
h Ru 3:10
i 1Sa 15:6; Met 19:22; Ho 6:6; Mik 6:8
j 1Sa 31:13
k 2Sa 15:20; Zb 40:11; Zb 57:3
l 2Sa 9:7; 2Sa 10:2; Met 11:10
m 2Sa 10:12
n Mwa 49:10; 2Sa 2:4
o 1Sa 14:50; 1Sa 17:55; 1Sa 26:5; 2Sa 4:1; 1Fa 2:5; 1Nya 26:28;
p 2Sa 3:7; 2Sa 4:5; 2Sa 4:12;
q Mwa 32:2; Yos 13:30; 2Sa 17:24;
r Hes 32:1; Yos 13:11;
s Yos 19:18;
t Yos 16:5;
u Yos 18:11;
v 2Sa 2:4.

11 Na hesabu ya siku ambazo
Daudi alikuwa mfalme katika
Hebroni juu ya nyumba ya Yuda
ikawa miaka saba na miezi sita.[a]

12 Baada ya muda Abneri
mwana wa Neri na watumi-
shi wa Ish-boshethi, mwana wa
Sauli, wakatoka Mahanaimu[b]
kwenda Gibeoni.[c] **13** Naye Yo-
abu[d] mwana wa Seruya[e] na wa-
tumishi wa Daudi wakaondoka
na baadaye wakakutana pamo-
ja kando ya kidimbwi cha Gi-
beoni; nao wakaendelea kuke-
ti, hawa upande huu wa kile ki-
dimbwi na wale upande ule
wa kile kidimbwi. **14** Mwisho-
we Abneri akamwambia Yoabu:
"Tafadhali, acha vijana wasima-
me, wapambane mbele yetu."
Naye Yoabu akasema: "Acha wa-
simame." **15** Basi wakasima-
ma, wakavuka kwa hesabu yao,
kumi na wawili wa Benyami-
ni na Ish-boshethi,[f] mwana wa
Sauli, na kumi na wawili ku-
toka kwa watumishi wa Dau-
di. **16** Ndipo wakaanza kuka-
matana kwa vichwa, huku upa-
nga wa kila mmoja ukiwa ka-
tika ubavu wa mwenzake, nao
wakaanguka pamoja. Na maha-
li hapo pakaitwa Helkath-hasu-
rimu, napo ni katika Gibeoni.[g]

17 Na mapigano yakawa ma-
gumu mno siku hiyo, na mwi-
showe Abneri[h] pamoja na
watu wa Israeli wakashindwa
mbele ya watumishi wa Dau-
di. **18** Basi wale wana watatu
wa Seruya[i] walikuwa hapo,
Yoabu[j] na Abishai[k] na Asahe-
li;[l] na Asaheli alikuwa mwepesi
kwa miguu yake, kama mmoja
wa swala[m] walio porini. **19** Na
Asaheli akamfuatilia Abneri,
naye hakwenda upande wa ku-
ume wala wa kushoto, aache
kumfuatilia Abneri. **20** Baa-
da ya muda Abneri akataza-
ma nyuma na kusema: "Je, ni
wewe, Asaheli?" naye akasema:
"Ni mimi." **21** Ndipo Abneri
akamwambia: "Geuka upande
wako wa kuume au wa kusho-
to, umkamate mmoja wa vija-
na awe wako na uchukue kile
utakachovua[a] kutoka kwake
kiwe chako." Na Asaheli haku-
taka kugeuka kando, aache ku-
mfuatilia. **22** Kwa hiyo Abne-
ri akamwambia tena Asahe-
li: "Geuza mwendo wako, acha
kunifuatilia. Kwa nini niku-
pige ufe na kuanguka chini?[b]
Hapo, basi, ningewezaje kuinua
uso wangu kumwelekea Yoabu
ndugu yako?" **23** Lakini aka-
endelea kukataa kugeuka ka-
ndo; ndipo Abneri akampiga tu-
mboni[c] kwa ncha ya nyuma ya
mkuki, hata mkuki ukatokea
upande wake wa nyuma; akaa-
nguka hapo, akafa papo hapo.
Na ikawa kwamba watu wote
waliofika mahali ambapo Asa-
heli alianguka kisha akafa wa-
kawa wakisimama tuli.[d]

24 Na Yoabu na Abishai wa-
kamfuatilia Abneri. Na jua lili-
pokuwa likitua wakafika katika
kilima cha Ama, kilicho mbele
ya Gia kwenye njia ya nyika ya
Gibeoni.[e] **25** Ndipo wana wa
Benyamini wakakusanyika nyu-
ma ya Abneri, wakawa kundi
moja, wakaendelea kusimama
juu ya kilima kimoja. **26** Ki-
sha Abneri akamwita Yoabu
na kusema: "Je, upanga uta-
kula[f] bila kukoma? Je, hujui
hakika kwamba uchungu ndio
utakaotokea mwishowe?[g] Basi,
itachukua muda gani kabla hu-
jawaambia watu warudi nyu-
ma, waache kuwafuatilia ndu-
gu zao?"[h] **27** Naye Yoabu aka-
sema: "Kama Mungu wa kweli
anavyoishi,[i] kama usingalise-
ma,[j] ni wakati wa asubuhi tu

SURA 2

a 2Sa 5:5
1Fa 2:11
1Nya 3:4
1Nya 29:27
b 2Sa 2:8
c Yos 10:1
Yos 10:12
Yos 18:25
Yos 21:17
2Sa 20:8
1Fa 3:5
1Nya 14:16
2Nya 1:3
Isa 28:21
d 2Sa 8:16
2Sa 20:23
1Fa 1:7
e 1Nya 2:16
f 2Sa 2:8
g 2Sa 2:12
h 2Sa 2:8
i 1Nya 2:16
j 2Sa 10:7
2Sa 18:2
2Sa 24:2
1Fa 11:15
1Nya 11:6
k 1Sa 26:6
2Sa 10:10
2Sa 20:6
1Nya 11:20
1Nya 19:11
l 2Sa 3:27
2Sa 23:24
1Nya 11:26
1Nya 27:7
m 1Nya 12:8
Wim 2:17
Wim 8:14

Safu ya 2

a Amu 14:19
2Nya 20:25
b Met 29:1
Mhu 6:10
c 2Sa 3:27
2Sa 4:6
2Sa 20:10
d 2Sa 20:12
e 2Sa 2:12
f 2Sa 11:25
Isa 1:20
Yer 2:30
Yer 12:12
Yer 46:10
g Met 17:14
h Mdo 7:26
i 1Sa 25:26
1Fa 2:24
2Fa 2:2
j Met 20:18
Lu 14:31

ndipo watu wangaliondolewa,
kila mmoja aache kumfuatilia
ndugu yake." **28** Basi Yoabu
akapiga baragumu,[a] kisha watu
wote wakasimama, wakaacha
kuwafuatilia Israeli, wala hawa-
kurudi tena kupigana upya.

29 Naye Abneri na watu
wake wakapiga mwendo ku-
pitia Araba[b] usiku huo wote,
wakavuka Yordani,[c] wakapiga
mwendo kuupitia mtaro mzima,
mwishowe wakafika Mahana-
imu.[d] **30** Naye Yoabu akageu-
ka, akaacha kumfuatilia Abne-
ri, akaanza kuwakusanya watu
wote pamoja. Na watumishi wa
Daudi walipungukiwa na watu
kumi na tisa pamoja na Asahe-
li. **31** Na watumishi wa Dau-
di walikuwa wamepiga watu wa
Benyamini na wa Abneri—wali-
kuwa watu 360 waliokufa.[e]
32 Nao wakamchukua Asahe-
li,[f] wakamzika katika kaburi
la baba yake,[g] katika Bethlehe-
mu.[h] Kisha Yoabu na watu wake
wakapiga mwendo usiku ku-
cha, na nuru ikawapambazukia
Hebroni.[i]

3 Na vita kati ya nyumba ya
Sauli na nyumba ya Dau-
di vikawa vya muda mrefu;[j] na
Daudi akazidi kupata nguvu,[k]
nayo nyumba ya Sauli ikazidi
kupungua.[l]

2 Wakati huo Daudi akazaa
wana[m] katika Hebroni,[n] na mza-
liwa wake wa kwanza aliku-
wa Amnoni[o] kupitia Ahinoamu[p]
mwanamke Myezreeli. **3** Na
mwana wake wa pili alikuwa Ki-
leabu[q] kupitia Abigaili[r] mke wa
Nabali Mkarmeli, na wa tatu ali-
kuwa Absalomu[s] mwana wa Ma-
aka binti ya Talmai[t] mfalme wa
Geshuri. **4** Na wa nne aliku-
wa Adoniya[u] mwana wa Hagi-
thi,[v] na wa tano alikuwa Shefa-
tia[w] mwana wa Abitali. **5** Na
wa sita alikuwa Ithreamu[a] ku-
pitia Egla, mke wa Daudi. Hao
ndio ambao Daudi alizaa katika
Hebroni.

6 Na ikawa kwamba vita kati
ya nyumba ya Sauli na nyumba
ya Daudi vilipokuwa vikiende-
lea, Abneri[b] alikuwa akiende-
lea kuimarisha cheo chake ka-
tika nyumba ya Sauli. **7** Basi
Sauli alikuwa na suria ambaye
jina lake lilikuwa Rispa,[c] binti
ya Aya.[d] Baadaye Ish-boshethi[e]
akamwambia Abneri: "Kwa nini
ulilala na suria[f] wa baba yangu?"
8 Ndipo Abneri akakasirika[g]
sana kwa sababu ya maneno ya
Ish-boshethi, akasema: "Je, mimi
ni kichwa cha mbwa[h] wa Yuda?
Leo ninaendelea kuonyesha fa-
dhili zenye upendo kwa nyu-
mba ya baba yako, kwa ndugu
zake na rafiki zake wa kibina-
fsi, nami sikukuacha uanguke
mkononi mwa Daudi; na bado
leo unanitoza hesabu kwa saba-
bu ya kosa linalohusu mwana-
mke. **9** Basi Mungu na amfa-
nyie Abneri hivyo, naye azidishe
jambo hilo,[i] ikiwa, kama vile Ye-
hova alivyomwapia Daudi,[j] sivyo
nitakavyomtendea, **10** ili kuuha-
misha ufalme kutoka katika
nyumba ya Sauli na kukiweka
kiti cha ufalme cha Daudi juu
ya Israeli na juu ya Yuda ku-
anzia Dani mpaka Beer-she-
ba."[k] **11** Naye hakuweza kuse-
ma hata neno moja zaidi ili ku-
mjibu Abneri, kwa sababu ya ku-
mwogopa.[l]

12 Papo hapo Abneri akatu-
ma wajumbe kwa Daudi, akise-
ma: "Je, nchi hii ni ya nani?" na
kuongezea: "Fanya agano lako
pamoja nami, na tazama! mko-
no wangu utakuwa pamoja nawe
ili kuwageuza Israeli wote wawe
upande wako."[m] **13** Naye aka-
sema: "Vema! Mimi nitafanya

SURA 2

a 1Sa 13:3
2Sa 18:16
2Sa 20:22
b Kum 1:7
Yos 12:3
c Mwa 32:10
Yos 4:1
d Mwa 32:2
Yos 21:38
2Sa 2:8
2Sa 17:24
e 2Sa 2:26
f 2Sa 2:18
1Nya 2:15
1Nya 2:16
g Mwa 47:30
Amu 8:32
Amu 16:31
2Sa 17:23
2Sa 19:37
h Mwa 35:19
Amu 17:7
Ru 1:19
Ru 4:11
1Sa 16:1
i 2Sa 2:1
2Sa 2:3
1Nya 11:1

SURA 3

j 1Fa 14:30
1Fa 15:16
k 1Sa 15:28
1Sa 24:20
1Sa 26:25
Ayu 17:9
l 2Sa 2:17
m Zb 127:3
n 1Nya 3:4
o 2Sa 13:1
p 1Sa 25:43
q 1Nya 3:1
r 1Sa 25:42
s 2Sa 15:12
t 2Sa 13:37
u 1Fa 1:5
v 1Nya 3:2
w 1Nya 3:3

Safu ya 2

a 1Nya 3:3
b 2Sa 2:8
c 2Sa 21:8
d 2Sa 21:11
e 2Sa 2:10
f 2Sa 16:21
2Sa 16:22
1Fa 2:22
Met 9:7
g Met 9:8
h 1Sa 17:43
1Sa 24:14
2Sa 16:9
i Ru 1:17
1Sa 3:17
1Sa 14:44
j 1Sa 15:28
1Sa 28:17
1Nya 12:23
Zb 78:70
Zb 89:20
k Amu 20:1
2Sa 17:11
2Sa 24:2
1Fa 4:25
l 2Sa 3:39
Met 29:25
m 2Sa 5:3
1Nya 11:3
Mdo 13:22

agano pamoja nawe. Ila tu kuna
jambo moja ambalo ninaomba
kwako, nikisema, 'Huwezi kuuona uso wangu,[a] isipokuwa kwanza umlete Mikali,[b] binti ya Sauli, utakapokuja kuuona uso
wangu.'" **14** Zaidi ya hayo, Daudi akatuma wajumbe kwa Ishboshethi,[c] mwana wa Sauli, akisema: "Mtoe mke wangu Mikali, niliyemchumbia kwa magovi[d]
mia moja ya Wafilisti." **15** Kwa
hiyo Ish-boshethi akatuma watu,
wakamchukua kutoka kwa
mume wake, Paltieli[e] mwana wa
Laishi. **16** Lakini mume wake
akaendelea kutembea pamoja
naye, akilia huku akimfuata
mpaka Bahurimu.[f] Ndipo Abneri akamwambia: "Nenda, rudi!"
Hivyo akarudi.

17 Wakati huo Abneri akawa amepashana habari na wanaume wazee wa Israeli, akisema: "Jana na juzi[g] pia mlikuwa
mkimtafuta Daudi awe mfalme
juu yenu. **18** Na sasa chukueni hatua, kwa maana Yehova
mwenyewe alimwambia Daudi,
'Kwa mkono wa Daudi[h] mtumishi wangu nitawaokoa watu wa
ngu Israeli kutoka katika mkono wa Wafilisti na kutoka katika mkono wa adui zao wote.'"
19 Kisha Abneri akasema pia
masikioni mwa Benyamini,[i] halafu pia Abneri akaenda kusema masikioni mwa Daudi kule
Hebroni yote yaliyokuwa mema
machoni pa Israeli na machoni
pa nyumba yote ya Benyamini.

20 Abneri alipokuja kwa Daudi kule Hebroni, na watu 20
pamoja naye, Daudi alimfanyia
Abneri karamu[j] na pia wale
watu waliokuwa pamoja naye.
21 Ndipo Abneri akamwambia
Daudi: "Niache niondoke, niende kukusanya pamoja Israeli wote kwa bwana wangu mfalme, ili wafanye agano pamoja nawe, nawe hakika utakuwa
mfalme juu ya wote ambao nafsi
yako inatamani."[a] Basi Daudi
akamwacha Abneri aende zake,
naye akaenda zake kwa amani.[b]

22 Na tazama, watumishi wa
Daudi na Yoabu walikuwa wa
kirudi kutoka kufanya uvamizi, na nyara[c] waliyoleta ilikuwa nyingi. Lakini Abneri hakuwa na Daudi katika Hebroni,
kwa maana alikuwa amemwacha aende zake, naye alikuwa
njiani akienda zake kwa amani.
23 Na Yoabu[d] na jeshi lote lililokuwa pamoja naye wakaingia,
nao wakampa Yoabu habari,
wakisema: "Abneri[e] mwana wa
Neri[f] alikuja kwa mfalme, naye
akamwacha aende zake, naye
yuko njiani anaenda zake kwa
amani." **24** Kwa hiyo Yoabu
akaingia kwa mfalme na kusema: "Umefanya nini?[g] Tazama!
Abneri amekuja kwako. Kwa
nini umemwacha aende zake,
akafanikiwa kwenda zake?
25 Unamjua vema Abneri mwana wa Neri, kwamba alikuja kukupumbaza, apate kujua kutoka kwako na kuingia kwako[h] na
kujua kila jambo unalofanya."[i]

26 Basi Yoabu akatoka mbele ya Daudi, akatuma wajumbe
wamfuate Abneri, nao wakamrudisha[j] akiwa kwenye tangi
la maji la Sira; na Daudi hakujua jambo hilo. **27** Abneri aliporudi Hebroni,[k] Yoabu akampeleka kando ndani ya lango
ili aseme naye kimyakimya.[l]
Hata hivyo, hapo akampiga tumboni,[m] hata akafa kwa sababu ya damu ya Asaheli[n] ndugu
yake. **28** Wakati Daudi aliposikia habari hizo baadaye, mara
moja akasema: "Kwa maoni
ya Yehova, mimi na ufalme wangu hatuna hatia ya damu[o] ya

SURA 3

a Mwa 43:3
Mwa 44:26
b 1Sa 18:20
1Sa 18:27
1Sa 19:11
1Sa 25:44
1Nya 15:29
c 2Sa 2:10
d 1Sa 18:25
1Sa 18:27
e 1Sa 25:44
f 2Sa 16:5
2Sa 17:18
1Fa 2:8
g 2Sa 5:2
1Nya 11:2
h 1Sa 13:14
1Sa 15:28
1Sa 16:1
1Sa 16:13
Zb 89:3
Zb 89:20
Zb 132:17
Mdo 13:22
i 1Sa 10:20
1Sa 10:21
1Nya 12:29
j Mwa 26:30

Safu ya 2

a Kum 14:26
1Fa 11:37
Zb 20:4
b Ro 12:18
c 1Sa 30:22
1Sa 30:24
d 2Sa 8:16
e 1Sa 14:50
1Sa 20:25
2Sa 2:8
2Sa 2:22
f 1Sa 14:51
g 2Sa 19:6
h Hes 27:17
Kum 28:6
1Sa 29:6
Zb 121:8
Isa 37:28
i Mwa 42:12
Mwa 42:16
j Met 26:24
k 2Sa 2:1
2Sa 3:20
l Zb 55:21
Met 26:23
Met 26:25
m Kum 27:24
1Fa 2:5
n 2Sa 2:22
2Sa 2:23
o Mwa 4:10
Mwa 9:6
Kut 21:12
Hes 35:21
Hes 35:33
Kum 21:9

Abneri mwana wa Neri mpaka
wakati usio na kipimo. **29** Na
ianguke na kurudi juu ya ki-
chwa[a] cha Yoabu na juu ya nyu-
mba yote ya baba yake, wala
asikose katika nyumba ya Yo-
abu[b] mwanamume anayetokwa
na mtiririko[c] au mwenye uko-
ma[d] au mwanamume anayeshi-
ka gurudumu linalozunguka la
kusokota nyuzi[e] au anayeangu-
ka kwa upanga au mwenye uhi-
taji wa mkate!"[f] **30** Na Yoabu
na Abishai[g] ndugu yake, wali-
muua Abneri[h] kwa sababu ali-
kuwa amemuua Asaheli ndugu
yao kule Gibeoni katika mapi-
gano.[i]

31 Kisha Daudi akamwa-
mbia Yoabu na watu wote wa-
liokuwa pamoja naye: "Rarueni
mavazi yenu,[j] na mvae nguo za
magunia,[k] mlie mbele ya Abne-
ri." Hata mfalme Daudi akate-
mbea nyuma ya kile kitanda.
32 Nao wakafanya mazishi ya
Abneri katika Hebroni; na mfa-
lme akapaaza sauti yake, aka-
lia kando ya kaburi la Abneri,
na watu wote wakalia.[l] **33** Na
mfalme akamwimbia Abneri na
kusema:

"Je, Abneri afe kifo kama
cha mtu asiye na akili?[m]
34 Mikono yako haikufungwa,[n]
Na miguu yako haikutiwa
katika pingu za shaba.[o]
Umeanguka kama yule
anayeanguka mbele ya
wana wa ukosefu wa
uadilifu."[p]

Ndipo watu wote wakamlilia[q]
tena.

35 Baadaye watu wote waka-
ja kumpa Daudi mkate[r] wa ku-
fariji siku ileile, lakini Dau-
di akaapa, akisema: "Mungu
na anifanyie hivyo[s] na kuzidi-
sha jambo hilo, nikionja mka-
te au kitu chochote kabla ya
jua kutua!"[a] **36** Na watu wote
wakaona, na jambo hilo likawa
jema machoni pao. Kama ilivyo
kwa kila jambo ambalo mfalme
alifanya, lilikuwa jema macho-
ni pa watu wote.[b] **37** Na watu
wote na Israeli wote wakajua
siku hiyo kwamba kuuawa kwa
Abneri mwana wa Neri hakuku-
tokana na mfalme.[c] **38** Na
mfalme akaendelea kuwaambia
watumishi wake: "Je, hamjui
kwamba ni mkuu na ni mtu
mkubwa ambaye ameanguka
katika Israeli leo?[d] **39** Nami
leo niko dhaifu ingawa nime-
tiwa mafuta[e] niwe mfalme, na
watu hawa, wana wa Seruya,[f]
ni wakali mno kwangu.[g] Yehova
na amlipe mwenye kufanya ma-
baya kulingana na ubaya wake
mwenyewe."[h]

4 Wakati mwana[i] wa Sauli
aliposikia kwamba Abne-
ri amekufa katika Hebroni,[j]
ndipo mikono yake ikalegea[k]
na Waisraeli wote wakavuru-
gika. **2** Na palikuwa na watu
wawili, wakuu wa vikundi vya
waporaji,[l] waliokuwa wa mwa-
na wa Sauli, jina la mmoja lili-
kuwa Baana na jina la mwingi-
ne lilikuwa Rekabu, wana wa
Rimoni Mbeerothi, wa wana wa
Benyamini; kwa maana Beero-
thi[m] pia lilikuwa likihesabiwa
kuwa sehemu ya Benyamini.
3 Na Wabeerothi wakakimbia
wakaenda Gitaimu,[n] nao waka-
wa wakaaji wageni hapo mpaka
leo hii.

4 Basi Yonathani,[o] mwana
wa Sauli, alikuwa na mwana
mwenye kulemaa miguu.[p] Ali-
kuwa na umri wa miaka mita-
no wakati habari juu ya Sauli na
Yonathani ilipofika kutoka Yez-
reeli;[q] na mlezi wake akamchu-
kua, akakimbia, lakini ikawa

SURA 3

a Kum 32:43
Amu 9:57
2Sa 1:16
1Fa 2:37
Zb 7:16
Zb 55:23
Zb 94:23
Met 5:22
Met 28:17
b Kut 34:7
c Law 15:2
Hes 5:2
d Law 13:44
2Fa 5:27
e Law 21:18
f Kum 27:24
Zb 109:10
g 2Sa 2:24
h 2Sa 2:8
2Sa 2:14
2Sa 3:27
i Law 19:18
2Sa 2:23
Ro 12:19
j Yos 7:6
2Sa 1:11
k Mwa 37:34
2Fa 19:1
l 1Sa 30:4
2Sa 1:12
m 2Sa 13:13
n Zb 107:10
o Amu 16:21
p 1Fa 2:32
q Mhu 7:2
r Yer 16:7
Eze 24:17
s Ru 1:17

Safu ya 2

a Amu 20:26
2Sa 1:12
b 2Sa 2:10
c 2Sa 3:28
1Fa 2:5
d 1Sa 14:50
2Sa 2:8
2Sa 3:12
e 2Sa 2:4
f 1Nya 2:16
g 2Sa 19:13
2Sa 20:10
2Sa 20:23
h 2Sa 3:29
1Fa 2:6
1Fa 2:34
Zb 28:4
Zb 62:12
Ga 6:7

SURA 4

i 2Sa 2:8
2Sa 3:7
j 2Sa 3:27
k 2Sa 17:2
Ezr 4:4
Isa 13:7
l 2Fa 5:2
2Fa 6:23
m Yos 9:17
Yos 18:25
n Ne 11:33
o 1Sa 20:16
p 2Sa 9:3
q 1Sa 29:1
1Sa 29:11

kwamba huyo mwanamke alipokuwa akikimbia akiwa na wasiwasi ili aponyoke, ndipo mtoto huyo akaanguka na kulemaa. Na jina lake lilikuwa Mefiboshethi.[a]

5 Na wana wa Rimoni Mbeerothi, Rekabu na Baana, wakaenda na kufika katika nyumba ya Ish-boshethi[b] mchana, wakati ambapo kulikuwa na joto jingi, alipokuwa analala usingizi wa mchana. **6** Nao wakaingia katika nyumba kama watu wanaochukua ngano, kisha wakampiga tumboni;[c] na Rekabu na Baana[d] ndugu yake wakakimbia bila kugunduliwa. **7** Wakati walipoingia katika ile nyumba, alikuwa amelala kitandani mwake katika chumba chake cha kulala cha ndani, ndipo wakampiga, wakamuua,[e] kisha wakakikata kichwa[f] chake na kukichukua, wakatembea barabarani mpaka Araba usiku kucha. **8** Mwishowe wakamletea Daudi kichwa cha Ish-boshethi,[g] akiwa Hebroni, wakamwambia mfalme: "Tazama, kichwa cha Ish-boshethi mwana wa Sauli adui[h] yako aliyeitafuta nafsi yako;[i] lakini leo hii Yehova amemlipizia kisasi[j] bwana wangu mfalme juu ya Sauli na uzao wake."

9 Hata hivyo, Daudi akawajibu Rekabu na Baana ndugu yake, wana wa Rimoni Mbeerothi, na kuwaambia: "Kama Yehova anavyoishi,[k] aliyeikomboa[l] nafsi[m] yangu kutoka katika kila taabu,[n] **10** mtu fulani aliponiletea habari,[o] akisema, 'Tazama, Sauli amekufa,' naye machoni pake mwenyewe akawa kama mtu anayeleta habari njema, hata hivyo, mimi nilimkamata nikamuua[p] katika Siklagi ingawa nilistahili kumpa ada ya mjumbe; **11** si zaidi sana wakati watu waovu[a] wamemuua mtu mwadilifu nyumbani mwake mwenyewe katika kitanda chake? Na je, sasa nisiitake damu yake kutoka mikononi mwenu,[b] na je, nisiwaondoe ninyi kutoka duniani?"[c] **12** Basi Daudi akawaamuru vijana, nao wakawaua,[d] wakaikata mikono yao na miguu yao na kuwatundika[e] kando ya kidimbwi kilicho katika Hebroni; nao wakakichukua kichwa cha Ish-boshethi, wakakizika katika kaburi la Abneri kule Hebroni.[f]

5 Baada ya muda makabila yote ya Israeli yakaja kwa Daudi[g] katika Hebroni[h] na kusema: "Tazama! Sisi ni mfupa wako na nyama yako.[i] **2** Jana na juzi vilevile,[j] Sauli alipokuwa mfalme juu yetu, ni wewe uliyeongoza Israeli katika kuwatoa na kuwaingiza.[k] Na Yehova alikuambia, 'Wewe utawachunga[l] watu wangu Israeli, nawe utakuwa kiongozi[m] juu ya Israeli.'" **3** Basi wanaume wote wazee[n] wa Israeli wakaja kwa mfalme katika Hebroni, na Mfalme Daudi akafanya agano[o] nao katika Hebroni mbele za Yehova; kisha wakamtia mafuta[p] Daudi awe mfalme juu ya Israeli.[q]

4 Daudi alikuwa na umri wa miaka 30 alipoanza kuwa mfalme. Akatawala kwa miaka 40[r] akiwa mfalme. **5** Katika Hebroni alitawala akiwa mfalme juu ya Yuda kwa miaka 7 na miezi 6;[s] na katika Yerusalemu[t] akatawala akiwa mfalme kwa miaka 33 juu ya Israeli yote na Yuda. **6** Basi mfalme na watu wake wakaenda Yerusalemu kupigana na Wayebusi[u] wanaokaa katika nchi, nao wakaanza kumwambia Daudi: "Wewe

SURA 4

a 2Sa 9:13
1Nya 8:34
1Nya 9:40
b 2Sa 2:8
2Sa 3:7
c 2Sa 2:23
2Sa 3:27
2Sa 20:10
d 2Sa 4:2
e 2Nya 24:25
2Nya 33:24
f 1Sa 17:54
1Sa 31:9
2Fa 10:6
Mk 6:28
g 2Sa 2:10
h 1Sa 18:11
1Sa 18:29
1Sa 19:2
i 1Sa 20:1
1Sa 20:33
1Sa 23:15
j Kum 32:35
2Sa 22:48
Ro 12:19
k 1Sa 20:3
l 1Sa 24:12
1Sa 26:25
2Sa 12:7
m Zb 71:23
n 1Fa 1:29
Zb 34:7
o 2Sa 1:2
p 2Sa 1:15

Safu ya 2

a 2Sa 4:5
1Fa 8:32
b Mwa 9:6
Kut 21:12
Hes 35:16
Hes 35:30
c Kut 9:15
Zb 109:15
d 2Sa 1:15
Zb 55:23
e Kum 21:22
f 2Sa 3:32

SURA 5

g 1Nya 11:1
1Nya 12:23
h 2Sa 2:1
2Sa 2:11
i Mwa 29:14
Kum 17:15
Amu 9:2
2Sa 19:12
j 2Sa 3:17
k Hes 27:17
1Sa 18:13
1Sa 25:28
l 1Sa 16:1
2Sa 7:7
Zb 78:71
m Mwa 49:10
1Sa 25:30
2Sa 6:21
2Sa 7:8
1Nya 28:4
n Kut 3:16
1Nya 11:3
o 2Fa 11:17
p 1Sa 16:13
2Sa 2:4
q Mdo 13:22
r 1Nya 29:27
s 2Sa 2:11
t Mwa 14:18
u Kut 23:23
Yos 15:63
Amu 1:8
Amu 1:21

hutaingia humu, lakini bila shaka vipofu na vilema watakufukuza,"[a] wao walikuwa wakifikiri: "Daudi hataingia humu."
7 Hata hivyo, Daudi akaiteka ngome ya Sayuni,[b] yaani, Jiji la Daudi.[c] **8** Hivyo Daudi akasema siku hiyo: "Yeyote atakayewapiga Wayebusi,[d] basi, kwa kutumia mfereji wa chini kwa chini wa maji,[e] na akutane na vilema pamoja na vipofu, wenye kuchukiza nafsi ya Daudi!" Ndiyo sababu wao husema: "Kipofu na kilema hawataingia katika nyumba." **9** Na Daudi akaanza kukaa katika ngome hiyo, nayo ikaitwa Jiji la Daudi; na Daudi akaanza kujenga kuzunguka pande zote kuanzia Kilima[f] na kuelekea ndani.
10 Kwa hiyo Daudi akaendelea kuwa mkuu zaidi na zaidi,[g] na Yehova Mungu wa majeshi[h] alikuwa pamoja naye.[i]

11 Na Hiramu[j] mfalme wa Tiro akatuma wajumbe[k] kwa Daudi, na pia mierezi[l] na wafanyakazi wa miti na wafanyakazi wa mawe ya kuta, nao wakaanza kumjengea Daudi nyumba.[m]
12 Na Daudi akajua kwamba Yehova alikuwa amemfanya imara kuwa mfalme juu ya Israeli[n] na kwamba alikuwa ameuinua[o] ufalme wake kwa ajili ya watu wake Israeli.[p]

13 Wakati huo Daudi akaendelea kuchukua masuria[q] na wake[r] zaidi kutoka katika Yerusalemu baada ya kutoka Hebroni; naye Daudi akaendelea kuzaa wana na mabinti zaidi.
14 Na haya ndiyo majina ya wale ambao alizaa katika Yerusalemu: Shamua[s] na Shobabu[t] na Nathani[u] na Sulemani,[v] **15** na Ibhari na Elishua[w] na Nefegi[x] na Yafia,[y]
16 na Elishama[z] na Eliada na Elifeleti.[a]

SURA 5

a Zb 5:5
b 1Nya 11:5
c 2Sa 12:28
1Fa 2:10
Ne 12:37
d 1Nya 11:6
e 2Fa 20:20
2Nya 32:30
f 1Fa 9:15
1Fa 9:24
1Fa 11:27
1Nya 11:8
2Nya 32:5
g 1Sa 16:13
2Sa 3:1
Ayu 17:9
h 1Sa 17:45
i Zb 46:7
Ro 8:31
j 1Fa 5:1
1Fa 5:8
1Nya 14:1
k 1Fa 20:9
l 2Nya 2:3
m 2Sa 7:2
n 2Sa 7:16
1Nya 14:2
Zb 41:11
Zb 89:21
o Zb 89:27
p 1Fa 10:9
2Nya 2:11
q Mwa 25:6
2Sa 15:16
1Nya 3:9
r 1Nya 14:3
s 1Nya 14:4
t 1Nya 3:5
u Zek 12:12
Lu 3:31
v 2Sa 12:24
w 1Nya 14:5
x 1Nya 14:6
y 1Nya 3:7
z 1Nya 14:7
a 1Nya 3:8

Safu ya 2

a 2Sa 5:3
1Nya 14:8
Zb 2:2
b 1Sa 22:1
1Sa 22:5
1Sa 24:22
2Sa 23:14
c Yos 15:8
1Nya 11:15
1Nya 14:9
Isa 17:5
d Hes 27:21
1Sa 23:2
2Sa 2:1
1Nya 14:10
Met 3:6
e Amu 20:28
1Sa 30:8
f 1Nya 14:11
g 2Sa 22:41
Zb 29:2
h 1Nya 14:11
Isa 28:21
i 1Sa 31:9
Zb 115:7
Isa 2:20
Hab 2:18
1Ko 8:4
j Kum 7:5
Kum 7:25
1Nya 14:12
k 1Nya 14:13
l Yos 15:8
2Sa 5:18
1Nya 11:15
m 1Sa 30:8
2Sa 5:19
Met 3:5

17 Na Wafilisti wakasikia kwamba walikuwa wamemtia mafuta Daudi awe mfalme juu ya Israeli.[a] Ndipo Wafilisti wote wakaja kumtafuta Daudi. Daudi aliposikia habari hizo, akashuka, akatoka na kwenda mahali palipo pagumu kufikiwa.[b]
18 Nao Wafilisti wakaingia na kuendelea kutembea huku na huku katika nchi tambarare ya chini ya Refaimu.[c] **19** Naye Daudi akaanza kumuuliza[d] Yehova, akisema: "Je, nipande kwenda kupigana na Wafilisti? Je, utawatia mkononi mwangu?" Ndipo Yehova akamwambia Daudi: "Panda uende, kwa maana bila shaka nitawatia Wafilisti mikononi mwako."[e] **20** Kwa hiyo Daudi akaja Baal-perasimu,[f] na Daudi akawapiga na kuwaua huko. Ndipo akasema: "Yehova amepenya katikati ya adui[g] zangu mbele yangu, kama pengo lililofanyizwa na maji." Ndiyo sababu alipaita mahali hapo jina Baal-perasimu.[h] **21** Basi wakaziacha sanamu[i] zao huko, kwa hiyo Daudi na watu wake wakazichukua.[j]

22 Baadaye Wafilisti wakaja tena[k] na kutembea huku na huku katika nchi tambarare ya chini ya Refaimu.[l] **23** Ndipo Daudi akamuuliza[m] Yehova, lakini yeye akasema: "Usipande kwenda. Zunguka uende nyuma yao, nawe uje juu yao mbele ya miti ya mibaka.[n] **24** Na iwe kwamba, utakaposikia sauti ya mwendo juu ya miti ya mibaka, ndipo utende bila kusita,[o] kwa sababu wakati huo Yehova atakuwa ametoka kwenda mbele yako kuipiga kambi ya Wafilisti."[p] **25** Basi Daudi akafanya hivyo, kama Yehova alivyo-

n 1Nya 14:14; Zb 84:6; o Amu 7:15; Yer 48:10; p 1Nya 14:15.

kuwa amemwamuru,[a] naye akawapiga[b] Wafilisti kutoka Geba[c] mpaka Gezeri.[d]

6 Na Daudi akawakusanya tena wanaume wote bora wa Israeli,[e] 30,000. **2** Kisha Daudi na watu wote waliokuwa pamoja naye wakaondoka, wakaenda Baale-yuda[f] ili kuleta kutoka hapo sanduku[g] la Mungu wa kweli, ambalo juu yake jina[h] limeitwa, jina la Yehova wa majeshi,[i] anayeketi juu ya makerubi.[j] **3** Hata hivyo, wakalipandisha sanduku la Mungu wa kweli juu ya gari jipya la kukokotwa,[k] ili walichukue kutoka katika nyumba ya Abinadabu,[l] iliyokuwa juu ya mlima; na Uza na Ahio,[m] wana wa Abinadabu, walikuwa wakiliongoza lile gari jipya.

4 Hivyo wakalichukua kutoka katika nyumba ya Abinadabu, iliyokuwa juu ya mlima —pamoja na sanduku la Mungu wa kweli; na Ahio alikuwa akitembea mbele ya lile Sanduku. **5** Na Daudi na nyumba yote ya Israeli walikuwa wakisherehekea mbele za Yehova kwa namna zote za vyombo vya mbao za mberoshi na kwa vinubi[n] na kwa vinanda[o] na kwa matari[p] na kwa matasa na kwa matoazi.[q] **6** Nao mwishowe wakaja mpaka uwanja wa kupuria wa Nakoni, na sasa Uza[r] akanyoosha mkono wake kwenye lile sanduku la Mungu wa kweli, akalishika,[s] kwa maana wale ng'ombe karibu waliangushe. **7** Ndipo hasira[t] ya Yehova ikamwakia Uza, na Mungu wa kweli akampiga[u] hapo kwa sababu ya hilo tendo lisilo la heshima kwa Mungu, naye akafa hapo karibu na lile sanduku la Mungu wa kweli.[v] **8** Na Daudi akakasirika kwa sababu Yehova alikuwa amemlipukia Uza, na mahali hapo pakaitwa Peres-uza mpaka leo hii.[a] **9** Naye Daudi akamwogopa Yehova[b] siku hiyo, akaanza kusema: "Sanduku la Yehova litakujaje kwangu?"[c] **10** Na Daudi hakutaka kulileta kwake sanduku la Yehova katika Jiji la Daudi.[d] Kwa hiyo Daudi akaagiza lipelekwe kando kwenye nyumba ya Obed-edomu,[e] Mgathi.[f]

11 Nalo sanduku la Yehova likaendelea kukaa katika nyumba ya Obed-edomu Mgathi miezi mitatu; na Yehova akazidi kumbariki[g] Obed-edomu na nyumba[h] yake yote. **12** Mwishowe Mfalme Daudi akaletewa habari, kusema: "Yehova ameibariki nyumba ya Obed-edomu na vitu vyake vyote kwa sababu ya lile sanduku la Mungu wa kweli." Kwa hiyo Daudi akaenda, akalitoa lile sanduku la Mungu wa kweli kutoka katika nyumba ya Obed-edomu, akaliweka katika Jiji la Daudi kwa kushangilia.[i] **13** Na ikawa kwamba wakati wachukuzi[j] wa lile sanduku la Yehova walipokuwa wamepiga hatua sita, akatoa mara moja dhabihu ya ng'ombe na kinono.[k]

14 Naye Daudi alikuwa anacheza dansi mbele za Yehova kwa nguvu zake zote, na wakati huo wote Daudi alikuwa amejifunga efodi[l] ya kitani. **15** Na Daudi na nyumba yote ya Israeli wakawa wanalipandisha sanduku[m] la Yehova kwa sauti za shangwe[n] na sauti za baragumu.[o] **16** Na ikawa kwamba wakati sanduku la Yehova lilipokuja ndani ya Jiji la Daudi, Mikali,[p] binti ya Sauli, akaangalia chini kutoka dirishani, akamwona Mfalme Daudi akiruka

SURA 5

a 1Nya 14:16
Zb 119:4
b Law 26:7
c Yos 18:24
d Yos 16:10

SURA 6

e 2Sa 5:1
1Fa 8:1
1Nya 13:1
f 1Sa 7:2
g 1Nya 13:6
h Kut 6:3
Law 24:11
Isa 42:8
i Kum 20:4
1Sa 1:3
1Sa 15:2
1Fa 18:15
1Nya 17:24
j Kut 25:22
1Sa 4:4
Zb 80:1
k Kut 25:14
Hes 7:9
Yos 3:14
l 1Sa 7:1
m 1Nya 13:7
n 1Sa 16:16
o 1Sa 10:5
Zb 150:3
p Kut 15:20
Zb 150:4
q 1Nya 13:8
Zb 150:5
r 1Nya 13:9
s Hes 4:15
Hes 4:19
Hes 4:20
1Nya 15:2
Met 11:2
Met 21:24
t Hes 12:9
2Fa 24:20
u Law 10:2
1Sa 6:19
v 1Nya 13:10

Safu ya 2

a 1Nya 13:11
b 1Sa 6:20
Zb 119:120
c 1Nya 13:12
d 2Sa 5:7
e 1Nya 13:14
1Nya 15:25
f 1Nya 13:13
g Mwa 30:27
Mwa 39:5
Met 10:22
Mal 3:10
h 1Nya 13:14
i 1Nya 15:25
Zb 24:7
Zb 68:24
j Hes 4:15
Hes 7:9
Yos 3:3
1Nya 15:2
1Nya 15:15
k 1Nya 15:26
l 1Sa 2:18
1Nya 15:27
m Kut 37:1
Zb 132:8
n 1Nya 15:16
1Nya 15:28
Zb 47:1
o 2Nya 15:14
Zb 150:3
p 1Sa 14:49
1Sa 18:20
1Sa 18:27
2Sa 3:14

na kucheza dansi huku na huku
mbele za Yehova; naye akaanza
kumdharau[a] moyoni[b] mwake.
17 Kwa hiyo wakaliingiza nda-
ni sanduku la Yehova na kuliwe-
ka mahali pake ndani ya hema
ambalo Daudi alikuwa amelisi-
mamishia;[c] kisha Daudi akatoa
dhabihu za kuteketezwa[d] na
dhabihu za ushirika[e] mbele za
Yehova. **18** Daudi alipomaliza
kutoa zile dhabihu za kuteke-
tezwa na dhabihu za ushirika,
akawabariki[f] watu katika jina
la Yehova[g] wa majeshi. **19** Za-
idi ya hayo, akawagawia[h] watu
wote, umati wote wa Israeli,
mwanamume na mwanamke vi-
levile, kila mmoja keki ya mka-
te ya mviringo na keki ya tende
na keki ya zabibu kavu,[i] kisha
watu wote wakaenda, kila mmo-
ja nyumbani kwake.

20 Basi Daudi akarudi kuwa-
bariki watu wa nyumba yake
mwenyewe,[j] na Mikali,[k] binti
ya Sauli, akatoka nje kumpo-
kea Daudi na kusema: "Lo! Ji-
nsi mfalme wa Israeli alivyoji-
tukuza leo[l] wakati alipojifunua
leo mbele ya macho ya vijakazi
wa watumishi wake, kama vile
mmoja wa watu wapumbavu
anavyojifunua!"[m] **21** Lakini
Daudi akamwambia Mikali: "Ili-
kuwa mbele za Yehova, aliye-
nichagua mimi badala ya baba
yako na nyumba yake yote,
akanipa amri[n] niwe kiongozi
juu ya Israeli, watu wa Yeho-
va, nami nitasherehekea mbele
za Yehova.[o] **22** Nami nitajipu-
uza hata zaidi kuliko hivi,[p] nita-
jishusha machoni pangu mwe-
nyewe; nami nimeamua kujitu-
kuza pamoja na wale vijakazi
uliowataja."[q] **23** Basi, kwa ha-
bari ya Mikali,[r] binti ya Sauli,
hakupata mtoto yeyote mpaka
siku ya kifo chake.

SURA 6

a 1Nya 15:29
b Yer 17:9
Mt 15:19
c 1Nya 15:1
1Nya 16:1
2Nya 1:4
d Law 1:3
e Law 3:1
Law 19:5
f 1Fa 8:55
hayo, alipotoa dhabihu, Absalo-
mu akatuma watu kumchukua
Ahithofeli[e] Mgiloni,[f] mshauri
wa Daudi,[g] kutoka katika Gilo[h]
jiji lake. Na hila[i] hiyo ikaende-
lea kupata nguvu, na hesabu ya
watu ikaendelea kuongezeka[j]
sikuzote kwa Absalomu.

13 Baada ya muda mleta-ha-
bari akaja kwa Daudi, akisema:
"Moyo[k] wa watu wa Israeli ume-
kuwa nyuma ya Absalomu."
14 Mara moja Daudi akawaam-
bia watumishi wake wote wa-
liokuwa pamoja naye katika
Yerusalemu: "Simameni, tuki-
mbie;[l] kwa maana hatutaponyo-
ka kwa sababu ya Absalomu!
Nendeni upesi, asije akaharaki-
sha, akatufikia na kututendea
mabaya na kulipiga jiji kwa
makali ya upanga!"[m] **15** Ndi-
po watumishi wa mfalme wa-
kamwambia mfalme: "Kulinga-
na na yote ambayo bwana wetu
mfalme atachagua, tazama, sisi
ni watumishi wako."[n] **16** Basi
mfalme akatoka, pamoja na
watu wote wa nyumbani mwa-
ke wakimfuata miguuni pake,[o]
na mfalme akawaacha wana-
wake kumi, masuria,[p] ili wai-
tunze nyumba. **17** Na mfalme
akaendelea kutoka pamoja na
watu wote wakimfuata miguu-
ni pake; nao wakaja kusimama
kule Beth-merhaki.

18 Na watumishi wake wote
walikuwa wakivuka kando yake;
na Wakerethi wote na Wape-
lethi[a] wote na Wagathi[b] wote,
watu mia sita waliokuwa wa-
memfuata kutoka Gathi,[c] wali-
kuwa wakivuka mbele ya uso
wa mfalme. **19** Ndipo mfalme
akamwambia Itai[d] Mgathi: "Kwa
nini wewe pia uende pamoja
nasi? Rudi,[e] ukae na mfalme;
kwa maana wewe ni mgeni, na
tena, wewe ni mhamishwa ku-
toka mahali pako. **20** Ulikuja
jana tu na je, leo nikufanye
utange-tange[f] pamoja nasi, ue-
nde wakati ninapoenda na po-
pote ninapoenda? Rudi, na uwa-
chukue ndugu zako urudi pamo-
ja nao, na Yehova akuonyeshe
fadhili zenye upendo[g] na uami-
nifu!"[h] **21** Lakini Itai akamji-
bu mfalme na kusema: "Kama
Yehova anavyoishi na kama ana-
vyoishi[i] bwana wangu mfalme,
mahali atakapokuwa bwana wa-
ngu mfalme, iwe ni kifo ama
ni uzima, hapo ndipo mtumishi
wako atakapokuwa!"[j] **22** Kwa
hiyo Daudi akamwambia Itai:[k]
"Nenda uvuke." Basi Itai Mga-
thi akavuka, na pia watu wake
wote na watoto wadogo wote
waliokuwa pamoja naye.

23 Na watu wote wa nchi wa-
kalia kwa sauti kubwa,[l] na watu
wote wakavuka, na mfalme ali-
kuwa amesimama kando ya bo-
nde la mto la Kidroni,[m] na watu
wote wakavuka kwenye bara-
bara pana inayoelekea nyika-
ni. **24** Na tazama, pia Sadoki[n]
alikuwapo na Walawi[o] wote pa-
moja naye wakiwa wamelichu-
kua[p] sanduku[q] la agano la Mu-
ngu wa kweli; nao wakaliwe-
ka chini sanduku la Mungu wa
kweli kando ya Abiathari[r] mpa-
ka watu wote walipomaliza ku-
vuka kutoka jijini. **25** Laki-
ni mfalme akamwambia Sadoki:
"Rudisha jijini[a] sanduku[b] la Mu-
ngu wa kweli. Nikipata kibali
machoni pa Yehova, hakika ata-
nirudisha na kuniruhusu nilio-
ne na pia makao yake.[c] **26** La-
kini akisema, 'Sikupendezwa
nawe,' basi, mimi hapa, na ani-
fanyie yaliyo mema machoni
pake."[d] **27** Na mfalme akaen-
delea kumwambia Sadoki ku-
hani: "Wewe ni mwonaji, sivyo?[e]
Rudi jijini kwa amani, na pia
Ahimaazi mwana wako na Yo-
nathani[f] mwana wa Abiathari,
wana wenu wawili, pamoja na-
nyi. **28** Tazama, nitangoja ka-
ndo ya vivuko vya nyikani mpa-
ka neno la kunipasha habari lije
kutoka kwenu."[g] **29** Basi Sa-
doki na Abiathari wakarudisha
sanduku la Mungu wa kweli Ye-
rusalemu, nao wakaendelea ku-
kaa huko.

30 Naye Daudi alikuwa aki-
panda kupitia mpando wa Mize-
ituni,[h] akilia alipokuwa akipa-
nda, kichwa chake kikiwa kime-
funikwa;[i] naye alikuwa akite-
mbea miguu wazi, na watu wote
waliokuwa pamoja naye waka-
funika vichwa vyao, kila mmo-
ja wao, wakapanda juu, wa-
kalia walipokuwa wakipanda.[j]
31 Na Daudi akaletewa habari,
iliyosema: "Ahithofeli yupo kati
ya wale wanaopanga hila[k] na
Absalomu."[l] Ndipo Daudi aka-
sema:[m] "Tafadhali, Ee Yehova,[n]
badili shauri la Ahithofeli liwe
upumbavu!"[o]

32 Na ikawa kwamba Daudi
alipofika kwenye kilele amba-
po kwa kawaida watu waliku-
wa wakimwinamia Mungu, ta-
zama, Hushai[p] Mwarki,[q] akij-
a kumpokea, kanzu yake ikiwa
imeraruliwa na kukiwa na vu-
mbi kichwani pake.[r] **33** Hata
hivyo, Daudi akamwambia:

SURA 15

a 2Sa 8:18
2Sa 20:7
1Fa 1:38
1Nya 18:17
b Yos 13:3
c 1Sa 27:4
1Nya 18:1
d 2Sa 18:2
e Ru 1:8
f Ebr 11:38
g Zb 25:10
Zb 57:3
Zb 61:7
Zb 85:10
Zb 89:14
h 2Sa 2:6
i 1Sa 20:3
1Sa 25:26
j Ru 1:17
Met 17:17
Met 18:24
Mt 8:19
k 2Sa 18:2
l Ro 12:15
m 1Fa 2:37
2Nya 30:14
Yoh 18:1
n 2Sa 8:17
2Sa 20:25
1Fa 1:8
1Fa 2:35
1Fa 4:2
1Nya 6:8
o Hes 8:19
1Nya 23:32
p Hes 4:15
Hes 7:9
1Sa 4:4
1Nya 15:2
q Kut 37:1
Law 16:2
r 1Sa 22:20
1Sa 30:7

Safu ya 2

a 2Sa 6:17
b 1Sa 4:3
c 2Sa 7:2
Zb 26:8
Zb 27:4
d 1Sa 3:18
1Pe 5:6
e 1Sa 9:9
2Nya 16:7
f 2Sa 17:17
g 2Sa 15:36
2Sa 17:16
2Sa 17:21
h Mt 21:1
Mt 24:3
Lu 19:29
Mdo 1:12
i Est 6:12
Yer 14:3
j Ro 12:15
k Zb 41:9
Zb 55:12
Mt 26:15
Yoh 13:18
l Zb 3:Uta
m Flp 4:6
n Zb 3:7
Zb 50:15
o 2Sa 16:23
2Sa 17:14
Ayu 12:20
1Ko 3:19
p 2Sa 16:16
q Yos 16:2
r 1Sa 4:12
2Sa 1:2

"Ukivuka kwenda pamoja
nami, hakika utakuwa mzigo
kwangu.[a] **34** Lakini ukirudi
jijini nawe umwambie Absalo-
mu, 'Mimi ni mtumishi wako,
Ee mfalme. Nilikuwa mtumishi
wa baba yako wakati ule, naam
mimi, lakini sasa mimi, naam
mimi, ni mtumishi wako,'[b] ndi-
po utavunja[c] shauri la Ahithofe-
li kwa ajili yangu. **35** Je, Sado-
ki na Abiathari, makuhani, ha-
wako huko pamoja nawe?[d] Na
itatukia kwamba kila jambo
ambalo huenda ukalisikia kuto-
ka katika nyumba ya mfalme,
utamwambia Sadoki na Abia-
thari, makuhani.[e] **36** Tazama!
Huko pamoja nao kuna wana
wao wawili, Ahimaazi[f] wa Sa-
doki na Yonathani[g] wa Abiatha-
ri; nanyi mwatumie hao kunile-
tea kila jambo ambalo huenda
mkalisikia." **37** Basi Hushai,
rafiki[h] ya Daudi, akaingia jijini.
Absalomu[i] naye akaingia Yeru-
salemu.

16 Daudi alipokuwa amevu-
ka mbele kidogo ya kile
kilele,[j] tazama, Siba[k] mtumi-
shi wa Mefiboshethi[l] alikuwa
akija kumpokea, akiwa na pu-
nda wawili[m] waliotandikwa,
na juu yao kulikuwa na mika-
te[n] mia mbili na keki mia moja
za zabibu kavu[o] na mizigo mia
moja ya matunda ya wakati
wa kiangazi[p] na mtungi mku-
bwa wa divai.[q] **2** Basi mfalme
akamwambia Siba: "Vitu hivi
vinamaanisha nini kwa upa-
nde wako?"[r] Ndipo Siba akase-
ma: "Hawa punda ni kwa ajili ya
nyumba ya mfalme ili wawapa-
nde, na hii mikate na mzigo wa
matunda ya wakati wa kiangazi
ni kwa ajili ya vijana[s] ili wale,
na divai ni kwa ajili ya mwenye
kuchoka[t] nyikani[u] ili anywe."
3 Mfalme akasema: "Na mwa-
na wa bwana wako yuko wapi?"[a]
Ndipo Siba akamwambia mfa-
lme: "Tazama, anakaa Yerusale-
mu; kwa maana alisema, 'Leo
nyumba ya Israeli watanirudi-
shia utawala wa kifalme wa
baba yangu.'"[b] **4** Basi mfalme
akamwambia Siba: "Tazama!
Mali yote ya Mefiboshethi ni
yako."[c] Na Siba akasema: "Mimi
ninainama.[d] Na nipate kibali
machoni pako, bwana wangu
mfalme."

5 Na Mfalme Daudi akaenda
mpaka Bahurimu,[e] na taza-
ma! palikuwa na mtu anato-
ka huko, wa familia ya nyu-
mba ya Sauli, na jina lake lili-
kuwa Shimei,[f] mwana wa Gera,
akiwa anatoka na kulaani huku
akiwa anatoka.[g] **6** Naye akaa-
nza kumtupia Daudi mawe, na
watumishi wote wa Mfalme Da-
udi; na watu wote na wanaume
wote wenye nguvu walikuwa
upande wake wa kuume na
wa kushoto. **7** Na Shimei akala-
aani akisema: "Ondoka, ondo-
ka, wewe mtu mwenye hatia ya
damu[h] na asiyefaa kitu![i] **8** Ye-
hova amerudisha juu yako hatia
yote ya damu kwa ajili ya nyu-
mba ya Sauli ambaye umetawa-
la ukiwa mfalme mahali pake; na
Yehova anautia ufalme mkono-
ni mwa Absalomu mwana wako.
Na sasa tazama, umo katika msi-
ba wako, kwa sababu wewe ni
mtu mwenye hatia ya damu!"[j]

9 Mwishowe Abishai mwana
wa Seruya[k] akamwambia mfa-
lme: "Kwa nini huyu mbwa
mfu[l] amlaani bwana wangu
mfalme?[m] Tafadhali acha nivu-
ke, niende nikiondoe kichwa
chake."[n] **10** Lakini mfalme
akasema: "Nina nini nanyi,[o]
enyi wana wa Seruya?[p] Mwa-
cheni alaani[q] hivyo, kwa saba-
bu Yehova amemwambia,[r] 'Mla-

SURA 15

a 2Sa 19:35
b 2Sa 16:19
c 2Sa 17:7
2Sa 17:14
d 2Sa 17:15
e 2Sa 17:16
f 2Sa 15:27
2Sa 18:19
g 2Sa 17:17
1Fa 1:42
h 2Sa 16:16
1Nya 27:33
Met 17:17
i 2Sa 16:15

SURA 16

j 2Sa 15:30
k 2Sa 9:2
2Sa 9:9
l 2Sa 9:6
m 1Sa 25:18
n 1Sa 17:17
2Sa 17:28
o 1Sa 30:12
p Yer 40:10
Amo 8:1
Mik 7:1
q 1Sa 10:3
r Met 17:8
Met 18:16
s 1Sa 25:27
t 2Sa 17:29
u 2Sa 15:23

Safu ya 2

a 2Sa 9:3
b Law 19:16
2Sa 19:27
Zb 15:3
Met 6:19
Met 26:22
c Kum 19:15
2Sa 9:10
d 2Sa 14:22
e 2Sa 3:16
1Fa 2:8
f 2Sa 19:16
1Fa 2:44
g Kut 22:28
1Sa 17:43
Met 1:22
Met 26:2
Mhu 10:20
Mdo 23:5
h 1Sa 24:6
1Sa 26:11
i Kum 13:13
1Sa 2:12
1Sa 25:17
Ayu 34:18
j Zb 3:1
Zb 3:2
Zb 7:1
Zb 71:11
k 1Nya 2:16
l 1Sa 24:14
2Sa 3:8
m Kut 22:28
Mdo 23:5
n 1Sa 26:8
Lu 9:54
Ro 12:19
o 2Sa 19:22
2Fa 3:13
Lu 9:55
p 1Fa 2:5
q Zb 37:8
1Pe 2:23
r 2Sa 12:10

ani Daudi!' Basi ni nani anayepaswa kusema, 'Kwa nini ulifanya hivyo?'"[a] **11** Na Daudi akaendelea kumwambia Abishai na watumishi wake wote: "Tazama, mwanangu mwenyewe, ambaye ametoka katika viuno vyangu, anaitafuta nafsi yangu;[b] si zaidi sasa Mbenyamini huyu![c] Mwacheni alaani, kwa maana Yehova amemwambia hivyo! **12** Labda Yehova atamona[d] kwa jicho lake, na Yehova atanirudishia wema badala ya laana yake leo hii."[e] **13** Kwa hiyo Daudi na watu wake wakazidi kusonga mbele barabarani, Shimei naye akiwa anatembea kando ya mlima, akitembea kando yake ili alaani;[f] naye akaendelea kutupa mawe akiwa kando yake, naye alitupa mavumbi mengi sana.[g]

14 Mwishowe mfalme na watu wote waliokuwa pamoja naye wakafika, wakiwa wamechoka. Basi wakajiburudisha huko.[h]

15 Lakini Absalomu na watu wote, wanaume wa Israeli, wakaingia Yerusalemu;[i] na Ahithofeli[j] alikuwa pamoja naye. **16** Na ikawa kwamba mara Hushai[k] Mwarki,[l] rafiki ya Daudi,[m] alipoingia kwa Absalomu, Hushai akamwambia Absalomu: "Mfalme na aishi![n] Mfalme na aishi!" **17** Ndipo Absalomu akamwambia Hushai: "Hizi ndizo fadhili zako zenye upendo kwa mwenzako, sivyo? Kwa nini hukuenda pamoja na mwenzako?"[o] **18** Kwa hiyo Hushai akamwambia Absalomu: "Sivyo; lakini yeye ambaye Yehova amemchagua na pia watu hawa na wanaume wote wa Israeli, nitakuwa wake, nami nitakaa pamoja naye. **19** Nami nitasema kwa mara ya pili, Mimi nitamtumikia nani? Je, si mbele ya mwana wake? Kama vile nilivyotumika mbele ya baba yako, ndivyo nitakavyokuwa mbele yako."[a]

20 Baadaye Absalomu akamwambia Ahithofeli: "Toeni shauri lenu.[b] Tufanye nini?" **21** Ndipo Ahithofeli akamwambia Absalomu: "Lala na masuria wa baba yako,[c] aliowaacha nyuma kuitunza nyumba.[d] Na Israeli wote hakika watasikia kwamba umenuka[e] mbele ya baba yako,[f] na mikono[g] ya wote walio pamoja nawe itapata nguvu." **22** Basi wakamsimamishia Absalomu hema juu ya dari,[h] naye Absalomu akaanza kulala na masuria wa baba yake[i] mbele ya macho ya Israeli wote.[j]

23 Na shauri la Ahithofeli, aliloshauri siku hizo, lilikuwa kama inavyokuwa wakati mtu ameuliza juu ya neno la Mungu wa kweli. Hivyo ndivyo lilivyokuwa shauri[k] lote la Ahithofeli[l] kwa Daudi na pia kwa Absalomu.

17 Naye Ahithofeli akamwambia Absalomu: "Tafadhali, acha nichague watu kumi na mbili elfu, niondoke na kumfuatilia Daudi usiku wa leo.[m] **2** Nami nitamfikia wakati yeye amechoka na mikono yake ina unyonge,[n] nami nitamtetemesha; na watu wote walio pamoja naye watakimbia, nami nitampiga na kumuua mfalme akiwa peke yake.[o] **3** Nami nitawarudisha kwako watu wote. Kurudi kwa watu wote kunategemea mtu unayemtafuta; na watu wote watakuwa na amani." **4** Na neno hilo likawa sawa machoni pa Absalomu[p] na machoni pa wanaume wazee wote wa Israeli.

SURA 16

a Ro 9:20
b 2Sa 12:11
2Sa 15:14
2Sa 17:12
c 2Sa 19:16
d Mwa 29:32
Kut 2:25
Kut 3:7
Zb 25:18
Met 15:3
e Kum 23:5
Zb 109:28
f Kut 22:28
2Sa 16:5
Mhu 10:20
g Mdo 22:23
h 2Sa 16:2
i 2Sa 15:37
j 2Sa 15:12
2Sa 15:31
k 2Sa 15:32
l Yos 16:2
m 2Sa 15:37
1Nya 27:33
n 1Sa 10:24
1Fa 1:25
2Fa 11:12
Da 2:4
o Mwa 26:26
1Fa 4:5
Met 17:17
Met 18:24

Safu ya 2

a 2Sa 15:34
Met 14:15
b Zb 37:12
Met 21:30
Isa 8:10
Mt 27:1
c Law 18:8
Law 20:11
2Sa 12:11
1Fa 2:22
Ayu 31:10
d 2Sa 15:16
e Mwa 34:30
1Sa 13:4
1Sa 27:12
f Mwa 49:4
g 2Sa 2:7
h 2Sa 11:2
i Kum 22:30
2Sa 12:11
2Sa 20:3
j Hes 25:6
2Sa 12:12
Isa 3:9
k 2Sa 17:14
l 2Sa 15:12
2Sa 17:23

SURA 17

m Met 1:16
Met 4:16
n Kum 25:18
2Sa 16:14
o 1Fa 22:31
Zb 37:12
Zb 41:9
Zb 55:12
p Mt 15:4
2Ti 3:3

5 Hata hivyo, Absalomu akasema: "Tafadhali, mwiteni Hushai[a] Mwarki, pia, nasi tusikie
maneno yaliyo kinywani mwake pia." **6** Basi Hushai akaingia kwa Absalomu. Ndipo
Absalomu akamwambia: "Ahithofeli amesema hivi na vile. Je, tutende kulingana na neno
lake? Ikiwa sivyo, wewe useme." **7** Ndipo Hushai akamwambia Absalomu: "Shauri ambalo Ahithofeli ametoa si jema wakati
huu!"[b]

8 Na Hushai akaendelea kusema: "Wewe mwenyewe unajua vema kwamba baba yako
na wanaume wake ni wenye nguvu,[c] nao wana uchungu wa nafsi,[d] kama dubu-jike ambaye
amepoteza watoto wake porini;[e] na baba yako ni shujaa wa vita,[f] naye hatalala usiku akiwa pamoja na watu. **9** Tazama! Sasa amejificha[g] katika
moja la mashimo au katika moja ya mahali penginepo; na hakika itatukia kwamba, mara ata-
kapowaangukia mwanzoni, yeye anayesikia hayo atayasikia na kusema, 'Watu wanaomfuata
Absalomu wameshindwa!' **10** Na hata mwanamume shujaa ambaye moyo wake ni kama
moyo wa simba[h] hakika atayeyuka katika udhaifu;[i] kwa maana Israeli wote wanajua kwa-
mba baba yako ni mwanamume mwenye nguvu[j] na pia wale wanaume mashujaa walio pamo-
ja naye.[k] **11** Mimi natoa shauri hili: Acha Israeli wote wakusanyike kwako bila kukosa,
kutoka Dani mpaka Beer-sheba,[l] kama mchanga ulio kando ya bahari kwa wingi,[m] nawe bi-
nafsi uende katika pigano.[n] **12** Nasi tuje juu yake katika moja ya mahali ambapo atapa-
tikana,[o] nasi tutakuja juu yake kama umande[a] unavyoanguka juu ya nchi; na hakika hata-
baki hata mmoja kati yake na watu wote walio pamoja naye. **13** Naye akiingia ndani ya jiji
fulani, Israeli wote watachukua kamba mpaka kwenye jiji hilo, nasi tutalivuta mpaka kwenye
bonde la mto, lisibaki hata jiwe moja humo."[b]

14 Ndipo Absalomu na watu wote wa Israeli wakasema: "Shauri la Hushai Mwarki ni
bora[c] kuliko shauri la Ahithofeli!" Na Yehova alikuwa ametoa amri[d] shauri la Ahithofeli livu-
njwe[e] ingawa lilikuwa jema,[f] ili Yehova alete msiba[g] juu ya Absalomu.

15 Baadaye Hushai akamwambia Sadoki[h] na Abiathari, makuhani: "Ahithofeli alimshau-
ri Absalomu na wanaume wazee wa Israeli hivi na vile; nami nikashauri hivi na vile. **16** Na
sasa tuma ujumbe haraka na umwambie Daudi,[i] ukisema, 'Usiku wa leo usilale katika
nchi tambarare za jangwa la nyikani, lakini wewe pia usikose kuvuka,[j] ili mfalme na watu
wote walio pamoja naye wasije wakamezwa.'"[k]

17 Kwa kuwa Yonathani[l] na Ahimaazi[m] walikuwa wamesimama katika En-rogeli,[n] mjaka-
zi fulani akaenda, akawaambia. Basi wakaondoka, kwa kuwa iliwapasa kumwambia Mfalme
Daudi; kwa maana haikuwezekana waonekane wakiingia jijini. **18** Hata hivyo, kijana
fulani akawaona, akamwambia Absalomu. Basi hao wawili wakaenda mbio, wakaja kwenye
nyumba ya mtu fulani katika Bahurimu,[o] aliyekuwa na kisima katika ua wake; nao waka-
shuka ndani ya kisima hicho. **19** Kisha yule mwanamke aka-

SURA 17

a 2Sa 15:32
2Sa 16:16
b 2Sa 15:34
c 1Sa 16:18
2Sa 15:18
2Sa 23:8
2Sa 23:18
1Nya 11:26
d Amu 18:25
e 2Fa 2:24
Met 17:12
Ho 13:8
f 1Sa 17:50
1Sa 18:7
1Sa 19:8
2Sa 10:18
g 1Sa 22:1
1Sa 23:19
h Mwa 49:9
Hes 24:9
2Sa 1:23
Isa 31:4
i Kum 1:28
Yos 2:9
Yos 7:5
1Sa 17:11
j 1Sa 18:5
Ebr 11:34
k 2Sa 17:8
l Amu 20:1
m Mwa 32:12
1Fa 4:20
n Zb 7:15
Zb 9:16
o 1Sa 23:23
2Sa 17:9

Safu ya 2

a Zb 110:3
b Mt 24:2
c Met 21:1
d Kum 2:30
2Nya 25:20
Zb 91:11
e 2Sa 15:31
2Sa 15:34
Ayu 5:12
Met 19:21
Met 21:30
Isa 8:10
1Ko 3:19
f 2Sa 16:23
g 1Sa 2:6
Ayu 34:11
Isa 46:10
h 2Sa 8:17
2Sa 15:35
1Nya 12:28
i 2Sa 15:28
j 2Sa 15:14
k 2Sa 20:19
Zb 35:25
l 2Sa 15:27
1Fa 1:42
m 2Sa 15:36
2Sa 18:19
n Yos 15:7
Yos 18:16
1Fa 1:9
o 2Sa 3:16
2Sa 16:5
2Sa 19:16

chukua kifuniko, akakitandaza
juu ya uso wa kile kisima na
kurundika juu yake nafaka ili-
yovunjwa;[a] wala halikujulika-
na jambo lolote. **20** Sasa wa-
tumishi wa Absalomu wakaja
kwa mwanamke yule nyumbani
kwake na kusema: "Ahimaazi
na Yonathani wako wapi?" Kwa
hiyo yule mwanamke akawaam-
bia: "Walipita hapa wakaen-
da kwenye maji."[b] Ndipo waka-
endelea kutafuta, nao hawaku-
wapata,[c] kisha wakarudi Yeru-
salemu.

21 Na ikawa kwamba baada
ya kuondoka kwao, ndipo wa-
katoka ndani ya kile kisima,
wakaenda, wakamweleza Daudi
na kumwambia Daudi: "Ondo-
keni, vukeni juu ya maji mbio-
mbio; kwa maana hivi ndivyo
Ahithofeli alivyotoa shauri[d]
juu yenu." **22** Mara moja Dau-
di akaondoka na pia watu wote
waliokuwa pamoja naye, nao
wakaendelea kuvuka Yordani
mpaka kulipopambazuka asu-
buhi,[e] mpaka kulipokuwa haku-
na hata mmoja ambaye hakuwa
amevuka Yordani.

23 Naye Ahithofeli akaona
kwamba haikutendwa kulinga-
na na shauri lake,[f] naye akata-
ndika punda, akaondoka na kwe-
nda nyumbani kwake katika jiji
lake.[g] Kisha akawapa nyumba
yake[h] amri halafu akajinyonga,[i]
akafa.[j] Basi akazikwa[k] katika
makaburi ya mababu zake.

24 Na Daudi akaja Maha-
naimu,[l] naye Absalomu aka-
vuka Yordani, yeye na watu
wote wa Israeli pamoja naye.
25 Na Amasa[m] ndiye ambaye
Absalomu aliweka mahali pa
Yoabu[n] juu ya jeshi; na Amasa
alikuwa mwana wa mtu ambaye
jina lake lilikuwa Ithra,[o] Mwi-
israeli, aliyelala na Abigaili,[p] bi-

SURA 17

a Yos 2:6
b Kut 1:19
Yos 2:5
1Sa 19:14
1Sa 21:2
Mt 10:16
c Yos 2:22
d 2Sa 17:2
e Met 27:12
f Met 16:18
g Yos 15:51
2Sa 15:12
h 2Fa 20:1
i Kut 20:13
1Sa 31:4
1Fa 16:18
Mt 27:5
Mdo 1:18
j Zb 5:10
Zb 55:23
k Mhu 8:10
l Mwa 32:2
Yos 13:26
2Sa 2:8
m 2Sa 19:13
2Sa 20:4
2Sa 20:10
n 2Sa 8:16
o 1Nya 2:17
p 1Nya 2:16

Safu ya 2

a Hes 32:1
Kum 3:15
b Kum 3:11
Yos 13:25
2Sa 12:29
c 2Sa 12:26
d 2Sa 9:4
e 2Sa 9:5
f 2Sa 19:32
1Fa 2:7
g 2Sa 19:31
h Mwa 18:6
1Sa 28:24
i 1Sa 25:18
j Eze 4:9
k Mwa 25:34
2Sa 23:11
l Kut 3:8
m Mwa 18:8
Met 30:33
n Met 11:25
Mdo 28:2
o 2Sa 16:2

SURA 18

p 1Sa 8:12
1Nya 13:1
1Ko 14:40
q Amu 7:16
Met 20:18
r 2Sa 8:16
2Sa 10:7
s 2Sa 23:18
t 1Nya 2:16
u 2Sa 15:19
2Sa 15:21
v 2Sa 21:17
w 2Sa 17:2
1Fa 22:31
x 2Sa 17:3
Omb 4:20
y Kut 17:10

nti ya Nahashi, dada ya Seruya,
mama ya Yoabu. **26** Na Israe-
li na Absalomu wakapiga kambi
katika nchi ya Gileadi.[a]

27 Na ikawa kwamba, mara
tu Daudi alipofika Mahanaimu,
Shobi mwana wa Nahashi ku-
toka Raba[b] la wana wa Amo-
ni,[c] na Makiri[d] mwana wa Ami-
eli[e] kutoka Lo-debari, na Barzi-
lai[f] Mgileadi, kutoka Rogelimu[g]
28 wakaleta vitanda na bese-
ni na vyombo vya mfinyanzi,
na ngano na shayiri na unga[h]
na nafaka iliyochomwa[i] na
maharagwe mapana[j] na dengu[k]
na nafaka iliyokauka; **29** na
asali[l] na siagi[m] na kondoo na
maziwa ya ng'ombe yaliyoga-
nda, wakaleta kwa ajili ya Dau-
di na kwa ajili ya watu waliooku-
wa pamoja naye ili wale,[n] kwa
maana walisema: "Watu wana
njaa nao wamechoka na wana
kiu nyikani."[o]

18 Na Daudi akawahesabu
watu waliokuwa pamoja
naye na kuweka juu yao wakuu
wa maelfu na wakuu wa ma-
mia.[p] **2** Na zaidi ya hayo, Da-
udi akapeleka sehemu ya tatu[q]
ya watu iwe chini ya mkono wa
Yoabu[r] na sehemu ya tatu chi-
ni ya mkono wa Abishai[s] mwana
wa Seruya, ndugu ya Yoabu,[t] na
sehemu ya tatu chini ya mkono
wa Itai[u] Mgathi. Kisha mfa-
lme akawaambia watu: "Mimi
pia hakika nitaenda pamoja na-
nyi." **3** Lakini watu wakase-
ma: "Usitoke kwenda nje,[v] kwa
maana tukikimbia, hawatawe-
ka moyo wao juu yetu;[w] na nusu
yetu tukifa, hawataweka moyo
wao juu yetu, kwa sababu tha-
mani yako ni kama elfu kumi
kati yetu;[x] na sasa ingekuwa
bora ututumikie kwa kutupa
msaada[y] ukiwa jijini." **4** Basi

mfalme akawaambia: "Lolote lililo jema machoni penu nitafanya."[a] Na mfalme akaendelea kusimama kando ya lango,[b] na watu wote wakatoka kwa mamia yao na kwa maelfu yao.[c]
5 Na mfalme akaendelea kuwaamuru Yoabu na Abishai na Itai, akisema: "Mtendeeni yule kijana Absalomu kwa upole[d] kwa ajili yangu." Na watu wote wakasikia mfalme alipowaamuru wale wakuu wote kuhusiana na jambo la Absalomu.

6 Na watu wakaendelea kwenda nje kukutana na Israeli; na pigano likawa katika msitu wa Efraimu.[e] **7** Mwishowe watu wa Israeli[f] wakashindwa[g] hapo mbele ya watumishi wa Daudi, na mauaji hapo yakawa makubwa siku hiyo, ya watu 20,000. **8** Na pigano hapo likaenea katika nchi yote yenye kuonekana. Zaidi ya hayo, huo msitu ulikula watu wengi kuliko wale walioliwa na upanga siku hiyo.

9 Mwishowe Absalomu akajikuta mbele ya watumishi wa Daudi. Na Absalomu alikuwa amepanda nyumbu, na yule nyumbu akaja chini ya mtandao wa matawi ya mti mkubwa mno, hivi kwamba kichwa chake kikakwama kabisa katika ule mti mkubwa, naye akainuliwa juu kati ya mbingu na dunia,[h] na yule nyumbu aliyekuwa chini yake akapita, akazidi kwenda mbele. **10** Ndipo mtu fulani akaona hayo, akamwambia Yoabu[i] na kusema: "Tazama! Nimemwona Absalomu akiwa amening'inia katika mti mkubwa." **11** Ndipo Yoabu akamwambia yule mtu aliyekuwa akimpasha habari: "Wewe uliona, kwa nini basi hukumpiga, aanguke chini hapo? Ndipo ningekuwa na wajibu wa kukupa vipande kumi vya fedha na mshipi."[a] **12** Lakini mtu huyo akamwambia Yoabu: "Hata kama mkononi mwangu ningekuwa na vipande elfu moja vya fedha, mimi singenyoosha mkono wangu juu ya mwana wa mfalme; kwa maana mfalme alikuamuru wewe na Abishai na Itai masikioni mwetu, akisema, 'Hata kama wewe ni nani, lindeni yule kijana, Absalomu.'[b] **13** Kama sivyo ningeitendea nafsi yake hila na mambo hayo yote hayangefichwa kutoka kwa mfalme,[c] nawe mwenyewe ungesimama kando." **14** Ndipo Yoabu akasema: "Acha nisijikawize hivi mbele yako!" Basi akachukua mkononi mwake mikuki midogo mitatu, akaichoma[d] ndani ya moyo wa Absalomu alipokuwa bado hai[e] katikati ya ule mti mkubwa. **15** Kisha watumishi kumi wenye kuchukua silaha za Yoabu wakaja, wakampiga Absalomu ili wamuue.[f] **16** Sasa Yoabu akapiga baragumu,[g] ili watu warudi, waache kufuatilia Israeli; kwa maana Yoabu alikuwa amewazuia watu. **17** Mwishowe wakamchukua Absalomu, wakamtupa msituni ndani ya shimo kubwa, wakarundika juu yake fungu kubwa sana la mawe.[h] Lakini Israeli wote wakakimbia, kila mtu akaenda nyumbani kwake.

18 Sasa Absalomu, alipokuwa angali hai, alikuwa amechukua na kujisimamishia nguzo,[i] ambayo ipo katika Nchi Tambarare ya Chini ya Mfalme,[j] kwa maana alisema: "Sina mwana ili kuweka jina langu katika kumbukumbu."[k] Basi akaiita nguzo hiyo kwa jina[l] lake mwe-

SURA 18
a Ru 3:5
Yak 3:17
b 2Sa 18:24
c 1Sa 29:2
d 2Sa 18:12
e 2Sa 17:26
f 2Sa 16:15
g 2Sa 2:17
2Nya 13:16
2Nya 28:6
Zb 3:7
Met 24:22
h 1Nya 21:16
i 2Sa 8:16
2Sa 18:2

Safu ya 2
a 1Sa 17:25
1Nya 11:6
b 2Sa 18:5
c Met 16:14
Met 24:21
d Amu 4:21
Amu 5:31
Zb 45:5
e 2Sa 18:9
f Kum 27:16
Kum 27:20
2Sa 12:10
Zb 63:9
Met 2:22
Met 20:20
Met 30:17
g 2Sa 2:28
h Yos 7:26
Yos 8:29
Yos 10:27
i 1Sa 15:12
j Mwa 14:17
k Hes 27:4
2Sa 14:27
l Zb 49:11

nyewe, nayo inaendelea kuitwa
Mnara wa Ukumbusho wa Absa-
lomu mpaka leo hii.
19 Naye Ahimaazi[a] mwana
wa Sadoki akasema: "Tafadha-
li, acha nikimbie, nimpelekee
mfalme habari hizi, kwa sababu
Yehova amemhukumu ili amwe-
ke huru kutoka mkononi mwa
adui zake."[b] **20** Lakini Yoabu
akamwambia: "Wewe si mtu wa
kupeleka habari leo, nawe uta-
peleka habari hizo siku nyi-
ngine; lakini leo usipeleke ha-
bari hizi, kwa sababu mwana
wa mfalme amekufa."[c] **21** Ndi-
po Yoabu akamwambia Mku-
shi:[d] "Nenda, mwambie mfalme
yale ambayo umeona." Kwa hiyo
yule Mkushi akamwinamia Yoa-
bu, akaanza kukimbia. **22** Basi
Ahimaazi mwana wa Sadoki aka-
mwambia tena Yoabu: "Tafadha-
li, sasa acha lolote litakalotokea
litokee, acha mimi pia nikimbie
nyuma ya yule Mkushi." Hata hi-
yo, Yoabu akasema: "Kwa nini
wewe ukimbie, mwanangu, na
hakuna habari zozote kwa aji-
li yako?" **23** Na bado akase-
ma: "Acha sasa litakalotokea li-
tokee, acha nikimbie." Basi aka-
mwambia: "Kimbia!" Ndipo Ahi-
maazi akaanza kukimbia kupitia
njia ya ile Wilaya,[e] na mwishowe
akampita yule Mkushi.
24 Basi Daudi alikuwa ame-
keti kati ya yale malango mawi-
li.[f] Na wakati huo mlinzi[g] akae-
nda juu ya paa ya lango kando ya
ukuta. Baada ya muda akainua
macho yake, akaona, na tazama!
palikuwa na mtu anakimbia aki-
wa peke yake. **25** Kwa hiyo
yule mlinzi akaita na kumwa-
mbia mfalme, kisha mfalme aka-
sema: "Ikiwa yuko peke yake,
kuna habari kinywani mwake."
Naye akazidi kuja, akaendelea
kusogea karibu. **26** Sasa mli-
nzi akaona mtu mwingine aki-
wa anakimbia. Kwa hiyo mli-
nzi akamwita mtunza-lango na
kusema: "Tazama! Mtu mwingi-
ne anakimbia akiwa peke yake!"
naye mfalme akasema: "Huyo
pia ni mleta-habari." **27** Na
mlinzi akaendelea kusema: "Ni-
naona kwamba namna ya kuki-
mbia ya yule wa kwanza ni kama
namna ya kukimbia[a] ya Ahi-
maazi[b] mwana wa Sadoki," naye
mfalme akasema: "Huyu ni mtu
mwema,[c] naye hakika anakuja
na habari njema."[d] **28** Mwi-
showe Ahimaazi akaita na ku-
mwambia mfalme: "Ni vema!"
Ndipo akamwinamia mfalme ki-
fudifudi. Naye akaendelea kuse-
ma: "Abarikiwe[e] Yehova Mungu
wako, ambaye amewatoa[f] watu
walionyoosha mkono wao juu ya
bwana wangu mfalme!"
29 Hata hivyo, mfalme aka-
sema: "Je, mambo ni mema kwa
yule kijana Absalomu?" Naye
Ahimaazi akasema: "Niliona
ghasia kubwa wakati Yoabu ali-
potuma mtumishi wa mfalme
na mtumishi wako, nami siku-
jua ni ya nini."[g] **30** Kwa hiyo
mfalme akasema: "Ondokea ka-
ndo, simama pale." Basi akao-
ndokea kando, akasimama tuli.
31 Na tazama, yule Mkushi[h]
akaingia, na huyo Mkushi akaa-
nza kusema: "Acha bwana wa-
ngu mfalme apokee habari, kwa
maana Yehova amekuhukumu
leo ili kukuweka huru kutoka
mkononi mwa wote wanaosima-
ma juu yako."[i] **32** Lakini mfa-
lme akamwambia Mkushi: "Je,
mambo ni mema kwa yule ki-
jana Absalomu?" Ndipo Mkushi
akasema: "Adui za bwana wa-
ngu mfalme na wote waliosima-
ma juu yako kwa uovu na wawe
kama yule kijana."[j]

SURA 18
a 2Sa 15:36
2Sa 17:17
b 2Sa 15:25
Zb 9:4
c 2Sa 18:5
d Mwa 10:6
Hes 12:1
2Nya 14:9
e 1Fa 7:46
2Nya 4:17
f 2Sa 18:4
g 2Sa 13:34
2Fa 9:17
Isa 21:6

Safu ya 2
a 2Fa 9:20
b 2Sa 18:19
c Met 25:13
d 1Fa 1:42
Met 25:25
e Mwa 14:20
2Sa 22:47
Zb 124:6
Zb 144:1
f 1Sa 26:8
Zb 31:8
g 2Sa 18:19
h 2Sa 18:21
i 2Sa 22:49
Zb 55:18
Zb 94:1
Zb 124:2
j Amu 5:31
Zb 27:2
Zb 68:1

33 Ndipo mfalme akahuzunika, akaenda juu katika chumba
cha dari[a] juu ya njia ya lango,
akaanza kulia; naye alisema
hivi akiwa anatembea: "Mwanangu Absalomu, mwanangu,
mwanangu[b] Absalomu! Laiti
mimi mwenyewe ningekufa badala yako, Absalomu mwanangu, mwanangu!"[c]

19 Baadaye Yoabu akaletewa habari hii: "Tazama!
Mfalme analia, naye anaendelea
kuomboleza juu ya Absalomu."[d]
2 Basi wokovu wa siku ile ukawa pindi ya watu wote kuomboleza, kwa sababu watu walisikia ikisemwa siku hiyo: "Mfalme ameona uchungu kwa sababu ya mwana wake." **3** Nao watu wakaanza kujificha na kuingia jijini siku hiyo,[e] kama vile watu wanavyojificha wakati wanapofedheheka kwa sababu ya kukimbia vitani. **4** Naye mfalme akajifunika uso, na mfalme akaendelea kulia kwa sauti kubwa: "Mwanangu Absalomu! Absalomu mwanangu, mwanangu!"[f]

5 Mwishowe Yoabu akaingia kwa mfalme nyumbani na kusema: "Leo umeaibisha uso wa watumishi wako wote, walioiokoa nafsi yako leo[g] na nafsi ya wana[h] wako na binti[i] zako na nafsi ya wake[j] zako na nafsi ya masuria wako,[k] **6** kwa kuwapenda wale wanaokuchukia na kuwachukia wale wanaokupenda; kwa maana leo umejulisha kwamba wakuu na watumishi si kitu kwako, kwa sababu mimi najua vema leo kwamba kama Absalomu angelikuwa hai na sisi sote wengine tungelikuwa wafu leo, basi hiyo ingelikuwa ni sawa machoni pako. **7** Na sasa ondoka, toka nje, useme moja kwa moja kwenye moyo[a] wa watumishi wako, kwa sababu mimi naapa kwa Yehova kwamba, usipotoka, hakuna hata mtu mmoja atakayebaki pamoja nawe usiku wa leo;[b] na jambo hilo kwa hakika litakuwa baya zaidi kwako kuliko madhara yote ambayo yamekupata kuanzia ujana wako mpaka sasa." **8** Basi mfalme akaondoka, akaketi langoni,[c] nao wakawapa watu wote habari hiyo, wakisema: "Tazama, mfalme ameketi langoni." Na watu wote wakaanza kuja mbele ya mfalme.

Lakini Israeli walikuwa wamekimbia kila mmoja kwenda nyumbani kwake.[d] **9** Na watu wote wakaja kuhusika katika ugomvi katika makabila yote ya Israeli, wakisema: "Mfalme ndiye aliyetuokoa kutoka mkononi mwa adui zetu,[e] na yeye ndiye aliyetuokoa mkononi mwa Wafilisti; na sasa amekimbia kutoka katika nchi mbele ya Absalomu.[f] **10** Naye Absalomu, tuliyemtia mafuta awe juu yetu,[g] amekufa vitani.[h] Basi sasa kwa nini hamfanyi lolote kumrudisha mfalme?"[i]

11 Basi Mfalme Daudi akatuma ujumbe kwa Sadoki[j] na Abiathari,[k] makuhani, akisema: "Semeni na wanaume wazee wa Yuda[l] hivi, 'Kwa nini ninyi muwe wa mwisho kumrudisha mfalme nyumbani kwake, wakati neno la Israeli wote limemfikia mfalme nyumbani kwake? **12** Ninyi ni ndugu zangu; ninyi ni mfupa na nyama yangu.[m] Basi kwa nini muwe wa mwisho kumrudisha mfalme?' **13** Nanyi mwambieni Amasa,[n] 'Je, wewe si mfupa wangu na nyama yangu? Basi Mungu na anifanyie hivyo na kuzidisha[o] jambo hilo ikiwa hutaku-

SURA 18
a 2Sa 18:24
b 2Sa 19:1
c 2Sa 12:10
2Sa 17:14
Met 10:1
Met 19:13

SURA 19
d 2Sa 18:5
2Sa 18:14
e 2Sa 17:24
2Sa 19:32
f 2Sa 18:33
g Zb 18:48
h 2Sa 3:3
2Sa 5:14
i 2Sa 13:1
j 2Sa 5:13
k 2Sa 15:16

Safu ya 2
a Isa 40:2
b Met 14:28
c 2Sa 18:4
2Sa 18:24
1Fa 22:10
Yer 38:7
d 2Sa 18:17
1Fa 22:36
e 1Sa 17:50
1Sa 18:7
1Sa 19:5
2Sa 5:25
2Sa 8:5
f 2Sa 15:14
g 2Sa 15:10
2Sa 15:12
h 2Sa 18:14
i 2Sa 3:17
j 2Sa 8:17
2Sa 15:25
1Fa 1:8
k 1Sa 22:20
1Sa 30:7
2Sa 15:24
1Nya 15:11
l 2Sa 2:4
m Amu 9:2
2Sa 5:1
n 2Sa 17:25
1Nya 2:17
o Ru 1:17
1Sa 3:17

wa mkuu wa jeshi mbele yangu
sikuzote badala ya Yoabu.'"[a]
14 Naye akaanza kuelekeza
moyo wa watu wote wa Yuda
wakawa kama mtu mmoja,[b] hivi
kwamba wakampelekea mfa-
lme neno hili: "Rudi, wewe na
watumishi wako wote."
15 Naye mfalme akaanza
kurudi, akafika Yordani. Nao
Yuda wakaja Gilgali[c] ili kwenda
kumpokea mfalme, wamvu-
she mfalme Yordani. **16** Ndi-
po Shimei[d] mwana wa Gera,[e]
Mbenyamini, aliyetoka Bahu-
rimu,[f] akafanya haraka, aka-
shuka pamoja na watu wa Yuda
ili kumpokea Mfalme Daudi.
17 Na palikuwa na watu 1,000
pamoja naye kutoka Benyami-
ni. (Na pia Siba[g] mtumishi wa
nyumba ya Sauli na wanawe
15[h] na watumishi wake 20 wali-
kuwa pamoja naye, nao wa-
kafaulu kufika Yordani mbe-
le ya mfalme. **18** Naye aka-
vuka kivuko[i] ili kuivusha nyu-
mba ya mfalme na kufanya
yaliyo mema machoni pake.)
Naye Shimei mwana wa Gera
akaanguka chini mbele ya
mfalme alipokuwa karibu ku-
vuka Yordani.[j] **19** Akamwa-
mbia mfalme: "Bwana wangu
asinihesabie kosa, nawe usiku-
mbuke kosa ambalo mtumishi
wako alifanya[k] siku ile bwana
wangu alipotoka Yerusalemu,
hivi kwamba mfalme aweke
hilo moyoni mwake.[l] **20** Kwa
maana mtumishi wako anajua
vema kwamba mimi ndiye nili-
yetenda dhambi; na kwa hiyo
leo mimi hapa nimekuja wa
kwanza kati ya nyumba yote ya
Yosefu[m] ili nishuke kumpokea
bwana wangu mfalme."
21 Mara moja Abishai,[n] mwa-
na wa Seruya,[o] akajibu na ku-
sema: "Je, Shimei hapaswi ku-
uawa kwa sababu hiyo, kwa
maana alimlaani mtiwa-mafuta
wa Yehova?"[a] **22** Lakini Dau-
di akasema: "Nina nini nanyi,[b]
ninyi wana wa Seruya, kwamba
muwe leo mpinzani[c] wangu? Je,
yeyote atauawa leo katika Isra-
eli?[d] Kwa maana, je, sijui vema
kwamba leo mimi ni mfalme
juu ya Israeli?" **23** Ndipo mfa-
lme akamwambia Shimei: "Hu-
takufa." Naye mfalme akamwa-
pia.[e]
24 Na Mefiboshethi[f] mjukuu
wa Sauli akashuka kuja ku-
mpokea mfalme; naye haku-
wa ametunza miguu[g] yake wala
kutunza masharubu[h] yake
wala kufua mavazi yake ta-
ngu siku ile mfalme alipoon-
doka mpaka siku ile alipoku-
ja kwa amani. **25** Na ikawa
kwamba alipokuja Yerusale-
mu kumpokea mfalme, ndipo
mfalme akamwambia: "Kwa
nini hukwenda pamoja nami,
Mefiboshethi?" **26** Naye aka-
sema: "Bwana wangu mfalme,
mtumishi wangu[i] ndiye aliye-
nidanganya. Kwa maana mtu-
mishi wako alikuwa amesema,
'Acha nijitandikie punda-jike
ili nimpande, niende pamoja na
mfalme,' kwa maana mtumi-
shi wako ni kilema.[j] **27** Kwa
hiyo akamchongea[k] mtumishi
wako kwa bwana wangu mfa-
lme. Lakini bwana wangu mfa-
lme ni kama malaika[l] wa Mu-
ngu wa kweli, na basi ufanye
yaliyo mema machoni pako.
28 Kwa maana nyumba yote
ya baba yangu ingelikuwa si
kitu ila kuhukumiwa kifo mbe-
le ya bwana wangu mfalme, na
hata hivyo ulimweka mtumishi
wako kati ya wale wanaokula
mezani pako.[m] Basi bado nina
nini kama dai la haki la kumli-
lia[n] zaidi mfalme?"

SURA 19
a 2Sa 8:16
2Sa 18:5
2Sa 18:14
b Amu 20:1
c Yos 5:9
1Sa 11:14
d 2Sa 16:5
1Fa 2:36
1Fa 2:44
e 1Fa 2:8
f 2Sa 3:16
2Sa 17:18
g 2Sa 9:2
2Sa 16:1
h 2Sa 9:10
i 2Sa 15:28
j Zb 66:3
Zb 81:15
Mhu 10:4
k 1Sa 26:21
2Sa 16:5
l 2Sa 13:20
2Sa 13:33
m 2Sa 19:43
1Nya 5:2
n 2Sa 23:18
o 2Sa 2:18

Safu ya 2
a Kut 22:28
2Sa 16:7
1Fa 21:13
Zb 105:15
Mhu 10:20
Mdo 23:5
2Pe 2:10
b 2Sa 3:39
2Sa 16:10
c 1Sa 29:4
1Fa 5:4
Mt 16:23
Yak 1:20
d 1Sa 11:13
e 1Fa 2:8
1Fa 2:37
1Fa 2:46
Ebr 6:16
f 2Sa 9:6
2Sa 16:4
g 2Sa 9:3
h Ezr 9:3
i 2Sa 9:9
j 2Sa 4:4
k Law 19:16
2Sa 16:3
Zb 101:5
Met 6:19
Met 21:6
l 1Sa 29:9
2Sa 14:17
m 2Sa 9:1
2Sa 9:7
2Sa 9:10
2Sa 9:13
n 2Sa 9:8

29 Hata hivyo, mfalme akamwambia: "Kwa nini bado
unaendelea kusema maneno yako? Mimi nasema, Wewe
na Siba mgawane hayo mashamba."[a] **30** Ndipo Mefibo-
shethi akamwambia mfalme:
"Acha ayachukue yote,[b] kwa
vile sasa bwana wangu mfalme
amekuja kwa amani nyumbani
kwake."
31 Naye Barzilai[c] Mgileadi
akashuka kutoka Rogelimu ili
apite mpaka Yordani pamoja
na mfalme, apate kumsindikiza
mpaka Yordani. **32** Na Bar-
zilai alikuwa mzee sana, akiwa
na umri wa miaka 80;[d] naye ali-
mwandalia mfalme chakula ali-
pokuwa akikaa Mahanaimu,[e]
kwa maana alikuwa mwana-
mume mkuu[f] sana. **33** Basi
mfalme akamwambia Barzi-
lai: "Wewe vuka pamoja nami,
nami nitakuandalia chakula
wewe pamoja nami katika Ye-
rusalemu."[g] **34** Lakini Barzi-
lai akamwambia mfalme: "Siku
za miaka ya maisha yangu ni
ngapi, ili kwamba niende Ye-
rusalemu pamoja na mfalme?
35 Mimi leo nina umri wa mia-
ka 80.[h] Je, ninaweza kutambua
kati ya jema na baya, au je, mtu-
mishi wako anaweza kuonja la-
dha ya kile ninachokula na kile
ninachokunywa,[i] au je, ninawe-
za kusikiliza[j] tena sauti za wai-
mbaji wa kiume na wa kike?[k]
Kwa nini basi mtumishi wako
awe mzigo[l] tena kwa bwana wa-
ngu mfalme? **36** Kwa maana
ni umbali kidogo tu ambao mtu-
mishi wako ameweza kumleta
mfalme mpaka Yordani, na kwa
nini mfalme anilipe thawabu
hii?[m] **37** Tafadhali, acha mtu-
mishi wako arudi, na acha nife[n]
katika jiji langu karibu na ka-
buri la baba yangu na mama
yangu.[a] Lakini, tazama, mtumi-
shi wako Kimhamu.[b] Acha avu-
ke pamoja na bwana wangu
mfalme; nawe umfanyie yaliyo
mema machoni pako."
38 Basi mfalme akasema:
"Kimhamu atavuka pamoja
nami, nami nitamfanyia yaliyo
mema machoni pako; na yote
ambayo utaamua kuweka juu
yangu nitakufanyia." **39** Sasa
watu wote wakaanza kuvuka
Yordani, naye mfalme akavu-
ka; lakini mfalme akambusu[c]
Barzilai na kumbariki,[d] kisha
akarudi mahali pake. **40** Mfa-
lme alipovuka kwenda Gilgali,[e]
Kimhamu alivuka pamoja naye,
na pia watu wote wa Yuda, na
pia nusu ya watu wa Israeli,
ili wamvushe mfalme.
41 Na, tazama! watu wote wa
Israeli walikuwa wakimjia mfa-
lme, nao wakamwambia mfa-
lme: "Kwa nini[f] ndugu zetu
watu wa Yuda walikuiba ili wa-
mlete mfalme na nyumba yake
na watu wote wa Daudi pa-
moja naye kuvuka Yordani?"[g]
42 Ndipo watu wote wa Yuda
wakawajibu watu wa Israeli:
"Kwa sababu mfalme ni mtu
wa karibu wa jamaa yetu;[h] na
kwa nini mmekasirika kwa ajili
ya jambo hili? Je, sisi tumekula
kwa gharama ya mfalme, au je,
tumepewa zawadi?"
43 Hata hivyo, watu wa Isra-
eli wakawajibu watu wa Yuda
na kusema: "Sisi tuna sehemu
kumi katika mfalme,[i] hivi kwa-
mba hata katika Daudi sisi ni
zaidi kuliko ninyi. Kwa nini,
basi, mmetutendea kwa dha-
rau, na kwa nini jambo letu ha-
likuwa la kwanza[j] sisi tumrudi-
she mfalme wetu?" Lakini neno
la watu wa Yuda likawa kali
zaidi kuliko neno la watu wa
Israeli.

SURA 19
a 2Sa 16:4
Met 18:17
Met 29:4
b Mt 5:40
1Ko 6:7
c 2Sa 17:27
1Fa 2:7
d Zb 90:10
e 2Sa 17:28
Met 3:27
Ebr 13:16
f 1Sa 25:2
Ayu 1:3
g 2Sa 9:10
Met 11:25
Mt 7:12
Lu 6:38
h Zb 90:10
i Mhu 8:15
Mhu 12:5
j Ayu 12:11
Mhu 12:4
k Ezr 2:65
Ne 7:67
Mhu 2:8
l 2Sa 13:25
2Sa 15:33
m Lu 6:38
n Yos 23:14
Lu 2:29

Safu ya 2
a Mwa 47:30
Mwa 49:29
Mwa 50:13
b 1Fa 2:7
c Mwa 31:55
Ru 1:14
1Sa 20:41
1Fa 19:20
Mdo 20:37
d Mwa 14:19
Mwa 47:7
Yos 22:6
e 1Sa 11:14
f Amu 8:1
Amu 12:1
g 2Sa 19:15
h Ru 4:12
Ru 4:22
2Sa 2:4
Zb 78:68
Mt 1:3
Mt 1:6
i 1Fa 11:31
1Fa 12:16
j Mhu 4:4
Lu 22:24
Lu 22:26
Ga 5:26
Flp 2:3

20 Basi palikuwa na mtu
asiyefaa kitu,[a] ambaye
jina lake lilikuwa Sheba,[b] mwa-
na wa Bikri, Mbenyamini; naye
akapiga baragumu[c] na kuse-
ma: "Hatuna fungu lolote ka-
tika Daudi, nasi hatuna uri-
thi wowote katika mwana wa
Yese.[d] Kila mmoja na aende
kwa miungu yake,[e] Ee Israeli!"
2 Basi watu wote wa Israeli
wakaanza kupanda, wakaacha
kumfuata Daudi ili wamfuate
Sheba mwana wa Bikri;[f] lakini
watu wa Yuda wakashikamana
na mfalme wao kutoka Yordani
mpaka Yerusalemu.[g]
3 Mwishowe Daudi akaja
nyumbani kwake katika Yeru-
salemu.[h] Ndipo mfalme akawa-
chukua wale wanawake kumi,[i]
masuria aliokuwa amewaacha
nyuma kuitunza nyumba, aka-
waweka katika nyumba ya uli-
nzi, lakini akaendelea kuwa-
pa chakula. Naye hakulala nao[j]
tena, lakini wakaendelea kufu-
ngiwa kabisa mpaka siku wali-
pokufa, wakiwa wajane wenye
mume aliye hai.
4 Basi mfalme akamwambia
Amasa:[k] "Wakusanye watu wa
Yuda waje kwangu katika muda
wa siku tatu, nawe usimame
hapa." **5** Kwa hiyo Amasa
akaenda kukusanya Yuda pa-
moja; lakini akaja baada ya
muda uliowekwa ambao aliku-
wa amemwekea. **6** Ndipo Da-
udi akamwambia Abishai:[l]
"Sasa Sheba[m] mwana wa Bi-
kri atakuwa mbaya kwetu ku-
liko Absalomu.[n] Wewe wachu-
kue watumishi[o] wa bwana
wako, umfuatilie, asije akajipa-
tia majiji yenye ngome na ku-
kimbia kutoka machoni petu."
7 Basi watu wa Yoabu[p] na Wa-
kerethi[q] na Wapelethi[r] na wana-
ume wote wenye nguvu wakato-
ka ili wamfuatilie; nao wakato-
ka nje ya Yerusalemu ili wamfu-
atilie Sheba mwana wa Bikri.
8 Walikuwa karibu na lile jiwe
kubwa lililo katika Gibeoni,[a]
naye Amasa[b] akaja kuwapo-
kea. Sasa Yoabu alikuwa ame-
jifunga, amevaa vazi; naye ali-
kuwa amefunga upanga kiu-
noni mwake, ukiwa katika ala
yake. Naye akaenda mbele, nao
ukaanguka.
9 Na Yoabu akamwambia
Amasa: "Je, mambo ni mema
kwako, ndugu yangu?"[c] Ndi-
po mkono wa kuume wa Yoa-
bu ukashika ndevu za Amasa
ili ambusu.[d] **10** Lakini Amasa
hakuwa mwangalifu juu ya ule
upanga uliokuwa mkononi mwa
Yoabu; naye akamchoma[e] nao
tumboni, na matumbo yake ya-
kamwagika chini, wala haku-
hitaji kurudia kufanya hivyo
tena. Basi akafa. Na Yoabu na
Abishai ndugu yake wakamfua-
tilia Sheba mwana wa Bikri.
11 Na mmoja wa vijana wa
Yoabu akasimama juu yake na
kusema: "Yeyote ambaye ame-
pendezwa na Yoabu na yeyo-
te ambaye ni wa Daudi,[f] na
amfuate Yoabu!" **12** Wakati
huo wote Amasa alikuwa aki-
gaagaa katika damu[g] katika-
ti ya njia kuu. Mtu yule alipo-
ona kwamba watu wote walisi-
mama tuli, akamwondoa Amasa
kutoka katika ile njia kuu mpa-
ka kwenye shamba. Mwisho-
we akamfunika vazi, kwa saba-
bu aliona kwamba kila mtu ali-
yefika kwake alisimama tuli.[h]
13 Mara tu alipokuwa ame-
mwondoa katika ile njia kuu,
kila mtu akapita, akimfuata Yo-
abu ili kumfuatilia Sheba[i] mwa-
na wa Bikri.
14 Na Sheba akapita kati ya
makabila yote ya Israeli mpaka

SURA 20
a Kum 13:13
1Sa 2:12
b 2Sa 20:21
c Amu 3:27
2Sa 15:10
d 2Sa 19:43
e Kum 13:6
Kum 13:9
1Fa 12:16
2Nya 10:16
f 2Sa 15:12
Met 6:19
Met 24:21
Ga 5:20
g 2Sa 19:15
2Sa 19:42
h 2Sa 5:11
i 2Sa 15:16
2Sa 16:21
j 2Sa 16:22
k 2Sa 17:25
2Sa 19:13
1Nya 2:17
l 1Sa 26:6
2Sa 10:10
2Sa 23:18
1Nya 11:20
1Nya 18:12
m 2Sa 20:1
n 2Sa 15:12
o 2Sa 11:11
1Fa 1:33
p 2Sa 8:16
q 2Sa 8:18
1Nya 18:17
r 2Sa 15:18
1Fa 1:38

Safu ya 2
a Yos 18:25
Yos 21:17
b 2Sa 17:25
2Sa 19:13
c Zb 55:21
Met 26:24
Mik 7:2
d Lu 22:47
e Hes 35:16
2Sa 3:27
1Fa 2:5
Zb 55:23
f 2Sa 20:2
2Sa 20:4
g Mwa 4:10
Mwa 9:5
h 2Sa 2:23
i 2Sa 20:1

jiji la Abeli la Beth-maaka.[a] Nao
Wabikri wote wakakutanika
pamoja, nao pia wakaingia nyu-
ma yake.
15 Nao wakaja, wakamzingi-
ra katika Abeli la Beth-maa-
ka, wakatengeneza boma la ku-
lizingira jiji hilo,[b] kwa kuwa li-
likuwa ndani ya boma. Na
watu wote waliokuwa pamo-
ja na Yoabu walikuwa wanau-
chimbua ukuta, ili kuubomoa.
16 Na mwanamke fulani mwe-
nye hekima[c] akaanza kuita
kutoka jijini: "Sikilizeni, siki-
lizeni! Tafadhali, mwambie-
ni Yoabu, 'Njoo karibu mpaka
hapa, nami niseme na wewe.'"
17 Basi akaenda karibu naye,
ndipo mwanamke huyo akasema:
"Je, wewe ni Yoabu?" naye
akasema: "Mimi ndiye." Ndipo
mwanamke huyo akamwambia:
"Yasikilize maneno ya kijakazi
wako."[d] Naye akasema: "Nina-
sikiliza." **18** Mwanamke huyo
akaendelea kusema: "Sikuzote
walikuwa wakisema katika nya-
kati za kale hivi, 'Na waulize
katika Abeli, na hakika ndi-
vyo watakavyolimaliza jambo
hili.' **19** Mimi nawakilisha we-
nye kufanya amani[e] na waa-
minifu[f] wa Israeli. Unatafuta
kuua jiji[g] na mama katika Isra-
eli. Kwa nini uumeze[h] urithi[i]
wa Yehova?" **20** Kwa hiyo Yo-
abu akajibu na kusema: "Ni ja-
mbo lisiloweza kuwaziwa kwa-
ngu, kwamba nimeze na ku-
haribu. **21** Jambo hili haliko
hivyo, lakini mtu fulani kuto-
ka eneo lenye milima la Efra-
imu,[j] ambaye jina lake ni She-
ba[k] mwana wa Bikri, amenyoo-
sha mkono wake juu ya Mfalme
Daudi.[l] Ninyi mtoeni yeye peke
yake,[m] nami nitaondoka juu ya
jiji hili."[n] Ndipo yule mwana-
mke akamwambia Yoabu: "Ta-

SURA 20
a 1Fa 15:20
2Fa 15:29
2Nya 16:4
b Mhu 9:14
Yer 33:4
Lu 19:43
c 1Sa 25:3
2Sa 14:2
d 1Sa 25:24
e Met 12:20
f Mwa 18:23
g Kum 20:10
h 2Sa 17:16
Zb 124:3
i Kut 19:5
Kum 32:9
2Sa 21:3
j Yos 17:15
Amu 2:9
k 2Sa 20:1
l 2Sa 20:6
m Hes 16:24
Yos 7:13
Met 17:11
n Hes 16:26

Safu ya 2
a 1Sa 17:51
1Sa 31:9
2Fa 10:7
b Mhu 9:15
Mhu 9:18
c 2Sa 2:28
2Sa 18:16
d 2Sa 8:16
2Sa 19:13
1Nya 18:15
e 2Sa 23:20
1Fa 1:38
1Nya 27:5
f 1Nya 12:27
g 2Sa 8:18
h 2Sa 15:18
1Fa 1:44
i 1Fa 4:6
1Fa 12:18
j 1Fa 4:3
k 1Nya 18:16
l 2Sa 8:17
m 2Sa 15:27
2Sa 17:15
1Fa 4:4
n 2Sa 19:11
o 1Nya 18:17

SURA 21
p Law 26:20
Kum 11:17
q Mwa 9:6
Kut 20:13
Kut 21:23
Hes 35:30
Hes 35:33
r Yos 9:3
Yos 9:17
Yos 9:27
s Mwa 10:16
Mwa 48:22
t Yos 9:15
u Eze 17:18
v Met 27:4
w Kut 32:30
Law 1:4
x 2Sa 20:19

zama! Utatupiwa kichwa chake[a]
kupitia ukutani!'"
22 Mara moja yule mwana-
mke akaenda kwa watu wote
kwa hekima yake,[b] nao waka-
kikata kichwa cha Sheba mwa-
na wa Bikri, wakamtupia Yoa-
bu. Basi akapiga baragumu,[c] nao
wakatawanyika kutoka kwenye
jiji lile, kila mmoja akaenda nyu-
mbani kwake; naye Yoabu aka-
rudi Yerusalemu kwa mfalme.
23 Na Yoabu alikuwa juu ya
jeshi[d] lote la Israeli; na Bena-
ya[e] mwana wa Yehoyada[f] aliku-
wa juu ya Wakerethi[g] na juu ya
Wapelethi.[h] **24** Na Adoramu[i]
alikuwa juu ya wale walioandi-
kishwa kufanya kazi ya kula-
zimishwa; na Yehoshafati[j] mwa-
na wa Ahiludi alikuwa karani.
25 Na Sheva[k] alikuwa mwandi-
shi,[l] na Sadoki[m] na Abiathari[n]
walikuwa makuhani. **26** Na
Ira, Myairi, pia akawa kuhani[o]
wa Daudi.

21 Basi kukawa na njaa[p] ka-
tika siku za Daudi kwa
miaka mitatu, mwaka baada ya
mwaka; naye Daudi akatafu-
ta shauri mbele za uso wa Ye-
hova. Kisha Yehova akasema:
"Kuna hatia ya damu juu ya
Sauli na juu ya nyumba yake,
kwa sababu aliwaua Wagibeo-
ni."[q] **2** Kwa hiyo mfalme aka-
waita Wagibeoni[r] na kuongea
nao. (Kama ilivyo, Wagibeoni
hawakuwa wa wana wa Israeli,
bali walikuwa mabaki ya Waa-
mori;[s] na wana wa Israeli wali-
kuwa wamewaapia,[t] lakini Sau-
li akatafuta kuwapiga[u] ili kuwa-
ua alipoona wivu[v] kwa sababu
ya wana wa Israeli na Yuda.)
3 Na Daudi akawaambia Wagi-
beoni: "Niwatendee nini, nami
nitafanya upatanisho[w] kwa ku-
tumia nini, ili muubariki uri-
thi[x] wa Yehova?" **4** Kwa hiyo

Wagibeoni wakamwambia: "Si jambo la fedha wala dhahabu[a] kwetu kwa habari ya Sauli na nyumba yake, wala si juu yetu kumuua mtu yeyote katika Israeli." Naye akasema: "Lolote mtakalosema nitawafanyia." **5** Ndipo wakamwambia mfalme: "Mtu aliyetuangamiza[b] na kupanga[c] kutumaliza tusiishi katika eneo lolote la Israeli, **6** na tupewe watu saba kati ya wanawe;[d] nasi tuwaweke mbele[e] za Yehova katika Gibea[f] la Sauli, aliyechaguliwa na Yehova."[g] Basi mfalme akasema: "Mimi mwenyewe nitawatoa."

7 Hata hivyo, mfalme akamhurumia Mefiboshethi[h] mwana wa Yonathani mwana wa Sauli kwa sababu ya kile kiapo[i] cha Yehova kilichokuwa kati yao, kati ya Daudi na Yonathani mwana wa Sauli. **8** Basi mfalme akawachukua wale wana wawili wa Rispa[j] binti ya Aya aliyemzalia Sauli, Armoni na Mefiboshethi, na wale wana watano wa Mikali[k] binti ya Sauli ambao alimzalia Adrieli[l] mwana wa Barzilai, Mmeholathi. **9** Ndipo akawatia mkononi mwa Wagibeoni, nao wakawaweka kwenye mlima mbele za Yehova,[m] hivi kwamba hao saba wakaanguka pamoja; nao waliuawa katika siku za kwanza za mavuno, mwanzoni mwa mavuno ya shayiri.[n] **10** Hata hivyo, Rispa binti ya Aya[o] akachukua nguo ya gunia,[p] akajitandikia juu ya mwamba tangu mwanzo wa mavuno mpaka maji yalipomwagika juu yao kutoka mbinguni;[q] naye hakuruhusu ndege[r] wa mbinguni watue juu yao wakati wa mchana wala wanyama wa mwituni[s] wakati wa usiku.

SURA 21

a Hes 35:31
b 2Sa 21:1
Mt 7:2
c Est 9:24
d Kum 19:21
Zb 9:12
e Mwa 40:19
Hes 25:4
Kum 21:22
f 1Sa 10:26
g 1Sa 9:17
h 2Sa 4:4
2Sa 9:10
2Sa 19:24
i 1Sa 18:3
1Sa 20:42
j 2Sa 3:7
k 1Sa 18:20
1Sa 25:44
2Sa 3:14
2Sa 6:23
l 1Sa 18:19
m Hes 35:31
Kum 19:21
1Sa 15:33
n Ru 1:22
o 2Sa 3:7
p 1Fa 21:27
Yoe 1:13
q Kum 11:14
Yer 5:24
r Mwa 40:19
s Eze 39:4

Safu ya 2

a Ru 2:11
b 1Sa 31:13
c 2Sa 2:5
d 1Sa 31:10
e 1Sa 31:12
f 1Sa 28:4
1Sa 31:1
2Sa 1:6
2Sa 1:21
1Nya 10:8
g 2Sa 21:9
h Yos 18:28
i 1Sa 9:1
1Sa 10:11
j Yos 7:26
2Sa 24:25
k 2Sa 5:17
2Sa 5:22
l Kum 2:11
m 1Sa 17:7
1Nya 11:23
n 2Sa 23:18
o 2Sa 22:19
p 2Sa 18:3
q 2Sa 14:7
r 1Fa 11:36
1Fa 15:4
2Fa 8:19

11 Mwishowe Daudi akaletewa habari[a] za mambo ambayo Rispa binti ya Aya, suria wa Sauli, alikuwa amefanya. **12** Kwa hiyo Daudi akaenda, akachukua mifupa ya Sauli[b] na mifupa ya Yonathani mwana wake kutoka kwa wenye mashamba wa Yabesh-gileadi,[c] ambao walikuwa wameiiba kutoka katika kiwanja cha watu wote cha Beth-shani,[d] mahali ambapo Wafilisti walikuwa wamewatundika[e] siku ambayo Wafilisti walimpiga na kumuua Sauli juu ya Gilboa.[f] **13** Naye akaleta kutoka huko mifupa ya Sauli na mifupa ya Yonathani mwana wake; tena wakaikusanya mifupa ya wale watu waliowekwa mbele zake.[g] **14** Kisha wakazika mifupa ya Sauli na Yonathani mwana wake katika nchi ya Benyamini huko Sela[h] katika kaburi la Kishi[i] baba yake, ili wafanye kila jambo ambalo mfalme alikuwa ameamuru. Basi Mungu akakubali kusihiwa kwa ajili ya nchi baada ya mambo hayo.[j]

15 Na Wafilisti[k] wakaja kupigana vita tena na Israeli. Basi Daudi na watumishi wake pamoja naye wakashuka na kupigana na Wafilisti; naye Daudi akachoka. **16** Na Ishbi-benobu, aliyekuwa mmoja wa wale waliozaliwa kwa Refaimu,[l] ambaye uzito wa mkuki[m] wake ulikuwa shekeli mia tatu za shaba na ambaye alikuwa amejifunga upanga mpya, akafikiria kumpiga na kumuua Daudi. **17** Basi Abishai[n] mwana wa Seruya akaja mara moja kumsaidia,[o] akampiga yule Mfilisti na kumuua. Ndipo watu wa Daudi wakamwapia, wakisema: "Usiende tena pamoja nasi vitani,[p] usije ukaizima[q] taa[r] ya Israeli!"

18 Na ikawa kwamba baada
ya hayo vita vikatokea tena na
Wafilisti katika Gobu. Ndipo Si-
bekai[a] Mhusha[b] akampiga Safu,
aliyekuwa mmoja wa wale wali-
ozaliwa kwa Refaimu.[c]
19 Na vita vikatokea tena na
Wafilisti katika Gobu, na Elha-
nani[d] mwana wa Yaare-oregimu
Mbethlehemu, akampiga Goliati
Mgathi, ambaye mpini wa
mkuki wake ulikuwa kama mti
wa wafumaji wa nguo.[e]
20 Na vita vikatokea tena
katika Gathi,[f] wakati kulipo-
kuwa na mtu mwenye ukubwa
usio wa kawaida, mwenye vi-
dole 6 katika kila mmoja wa
mikono yake na vidole 6 kati-
ka kila mmoja wa miguu yake,
jumla yake 24; naye pia ali-
kuwa amezaliwa kwa Refaimu.[g]
21 Naye akaendelea kudhihaki[h]
Israeli. Mwishowe Yonatha-
ni[i] mwana wa Shimei,[j] ndugu ya
Daudi, akampiga na kumuua.
22 Hao wanne walikuwa wa-
mezaliwa kwa Refaimu katika
Gathi;[k] nao wakaanguka kwa
mkono wa Daudi na kwa mkono
wa watumishi wake.[l]

22 Na Daudi akamwambia
Yehova maneno ya wi-
mbo[m] huu siku ambayo Yeho-
va alikuwa amemkomboa kuto-
ka katika mkono wa adui[n] zake
wote na kutoka katika mkono
wa Sauli;[o] **2** naye akasema:
"Yehova ni mwamba[p]
wangu na ngome[q] yangu
na Mwokoaji wangu.[r]
3 Mungu wangu ni mwamba[s]
wangu. Nitamkimbilia,
Ngao[t] yangu na pembe[u]
yangu ya wokovu, kilele[v]
changu salama,
Na mahali pangu pa
kukimbilia,[w] Mwokozi[x]
wangu; unaniokoa
kutoka katika jeuri.[y]
4 Nitamwita, Yehova, Yule
anayestahili kusifiwa,[a]
Nami nitaokolewa kutoka
kwa adui zangu.[b]
5 Kwa maana mashuu
yanayosababisha kifo
yalinizunguka;[c]
Kulikuwa na mafuriko ya
ghafula ya watu wasiofaa
kitu yaliyoendelea
kuniogopesha.[d]
6 Kamba za Kaburi*
zilinizunguka;[e]
Mitego ya kifo ilinikabili.[f]
7 Katika taabu yangu
niliendelea kumwita
Yehova,[g]
Nami niliendelea kumwita
Mungu wangu.[h]
Ndipo kutoka katika
hekalu lake akaisikia
sauti yangu,[i]
Kilio changu cha kuomba
msaada kikaingia
masikioni mwake.[j]
8 Nayo dunia ikaanza
kutikisika na
kutetemeka;[k]
Misingi ya mbingu
ikasukasuka,[l]
Nayo ikatikisika-tikisika
kwa sababu alikuwa
amekasirishwa.[m]
9 Moshi ukapanda katika
mianzi ya pua yake, na
moto kutoka kinywani
mwake ukaendelea
kuteketeza;[n]
Makaa yakawaka moto
kutoka kwake.[o]
10 Naye akaziinamisha
mbingu, akashuka;[p]
Na giza zito lilikuwa chini
ya miguu yake.[q]
11 Naye akaja akiwa
amepanda juu ya kerubi,[r]
akaja akiwa anaruka;

SURA 21
a 1Nya 11:29 1Nya 20:4 1Nya 27:11
b 2Sa 23:27
c Mwa 14:5 2Sa 21:16
d 1Nya 20:5
e 1Sa 17:7
f 1Nya 20:6
g 2Sa 21:16
h 1Sa 17:10 1Sa 17:45 2Fa 19:22
i 1Nya 20:7
j 1Sa 16:9 1Sa 17:13 1Nya 2:13
k 1Nya 20:8
l Zb 60:12 Zb 108:13 Eze 32:27

SURA 22
m Kut 15:1 Amu 5:1
n Zb 18:Uta Zb 34:19
o 1Sa 23:14
p Zb 18:2
q Zb 31:3
r Zb 144:2
s Kum 32:4 1Sa 2:2 Zb 144:1
t Mwa 15:1 Kum 33:29 Zb 3:3
u 1Sa 2:1
v Zb 9:9 Zb 18:2 Zb 61:3 Met 18:10
w Zb 59:16 Yer 16:19
x Isa 12:2 Lu 1:47 Tit 3:4
y Zb 72:14

Safu ya 2
a Zb 148:1
b Zb 18:3
c Zb 69:14
d Zb 18:4
e Zb 116:3
f Zb 18:5
g Zb 120:1 Zb 142:1 Yon 2:2
h Zb 116:4
i Zb 18:6
j Kut 3:7 Zb 34:15
k Amu 5:4
25 Naye Nadabu[a] mwana wa Yeroboamu akawa mfalme juu ya Israeli katika mwaka wa pili wa Asa mfalme wa Yuda; naye akaendelea kutawala juu ya Israeli miaka miwili. **26** Naye akaendelea kutenda yaliyokuwa mabaya[b] machoni pa Yehova, akaendelea kutembea katika njia ya baba yake[c] na katika dhambi yake ambayo kwa hiyo alisababisha Israeli kutenda dhambi.[d] **27** Na Baasha[e] mwana wa Ahiya wa nyumba ya Isakari akaanza kupanga hila juu yake; naye Baasha akampiga na kumuua kule Gibethoni,[f] jiji la Wafilisti, wakati Nadabu na Israeli wote walipokuwa wakilizingira Gibethoni. **28** Kwa hiyo Baasha akamuua katika mwaka wa tatu wa Asa mfalme wa Yuda, akaanza kutawala mahali pake.[g] **29** Na ikawa kwamba mara tu alipokuwa mfalme, akaipiga nyumba yote ya Yeroboamu. Hakuacha yeyote wa Yeroboamu anayepumua abaki mpaka alipokuwa amewaangamiza, kulingana na neno la Yehova alilosema kupitia mtumishi wake Ahiya Mshilo,[h] **30** kwa sababu ya dhambi za Yeroboamu ambazo kupitia hizo alisababisha Israeli kutenda dhambi[i] na kwa kutia uchungu kwake alikomtia uchungu Yehova Mungu wa Israeli.[j] **31** Na mambo mengine ya Nadabu na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa katika kitabu[k] cha mambo ya siku za wafalme wa Israeli? **32** Na vita vikatokea kati ya Asa na Baasha mfalme wa Israeli siku zao zote.[l]

33 Katika mwaka wa tatu wa Asa mfalme wa Yuda, Baasha mwana wa Ahiya akawa mfalme juu ya Israeli yote kule

Tirsa kwa miaka 24.[a] **34** Naye akaendelea kutenda yaliyokuwa mabaya machoni pa Yehova,[b] akaendelea kutembea katika njia ya Yeroboamu[c] na katika dhambi yake ambayo kupitia hiyo alisababisha Israeli kutenda dhambi.[d]

16 Ndipo neno la Yehova likamjia Yehu[e] mwana wa Hanani[f] juu ya Baasha, akisema: **2** "Kwa vile nilikusimamisha kutoka mavumbini[g] ili nikufanye kiongozi juu ya watu wangu Israeli,[h] lakini ukaanza kutembea katika njia ya Yeroboamu[i] na hivyo kusababisha watu wangu Israeli watende dhambi kwa kunitia uchungu kwa dhambi zao,[j] **3** tazama, ninafagia kabisa nikimfuata Baasha na nyumba yake, nami nitaifanya nyumba yake iwe kama nyumba ya Yeroboamu mwana wa Nebati.[k] **4** Mtu yeyote wa Baasha anayekufa jijini mbwa watamla; na mtu wake yeyote anayekufa shambani ndege wa mbinguni watamla."[l]

5 Na mambo mengine ya Baasha na yale aliyoyafanya na nguvu zake, je, hayakuandikwa katika kitabu[m] cha mambo ya siku za wafalme wa Israeli? **6** Mwishowe Baasha akalala pamoja na mababu zake, akazikwa kule Tirsa;[n] na Ela mwana wake akaanza kutawala mahali pake. **7** Na pia kupitia Yehu mwana wa Hanani nabii, neno la Yehova lilikuja juu ya Baasha na nyumba yake,[o] kwa sababu ya ubaya wote aliotenda machoni pa Yehova kwa kumtia uchungu[p] kwa kazi za mikono yake,[q] ili iwe kama nyumba ya Yeroboamu, na pia kwa sababu alimpiga na kumuua.[r]

8 Katika mwaka wa 26 wa Asa mfalme wa Yuda, Ela mwana wa Baasha akawa mfalme juu ya Israeli kule Tirsa kwa miaka miwili. **9** Na Zimri[a] mtumishi wake, mkuu wa nusu ya magari, akaanza kupanga hila juu yake, alipokuwa kule Tirsa akinywa[b] na kulewa nyumbani kwa Arsa, aliyekuwa juu ya nyumba[c] kule Tirsa. **10** Na Zimri akaingia, akampiga na kumuua[d] katika mwaka wa 27 wa Asa mfalme wa Yuda, naye akaanza kutawala mahali pake. **11** Na ikawa kwamba wakati alipoanza kutawala, mara tu alipoketi katika kiti chake cha ufalme, akaipiga nyumba yote ya Baasha. Hakuacha abaki mtu yeyote wa kwake anayekojoa ukutani[e] wala walipiza-kisasi wake wa damu[f] wala rafiki zake. **12** Hivyo ndivyo Zimri alivyoiangamiza nyumba yote ya Baasha,[g] kulingana na neno la Yehova[h] alilokuwa amesema juu ya Baasha kupitia Yehu nabii,[i] **13** kwa sababu ya dhambi zote za Baasha na dhambi za Ela[j] mwana wake ambazo walitenda na ambazo kupitia hizo walisababisha Israeli kutenda dhambi kwa kumtia uchungu Yehova Mungu wa Israeli, kwa sanamu zao za ubatili.[k] **14** Na mambo mengine ya Ela na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa katika kitabu[l] cha mambo ya siku za wafalme wa Israeli?

15 Katika mwaka wa 27 wa Asa mfalme wa Yuda, Zimri akawa mfalme kwa siku 7[m] kule Tirsa, watu walipokuwa wamepiga kambi juu ya Gibethoni,[n] jiji la Wafilisti. **16** Baada ya muda watu waliokuwa wamepiga kambi wakasikia habari, zikisema: "Zimri amepanga hila na pia akampiga na kumuua mfalme." Basi Israeli wote

SURA 15

a 1Fa 16:8
b 1Fa 16:7
c 1Fa 12:28
1Fa 13:33
d 1Fa 14:9
Isa 1:4

SURA 16

e 2Nya 19:2
2Nya 20:34
f 2Nya 16:7
g 1Sa 2:8
Zb 113:7
h Zb 75:7
Lu 1:52
i 1Fa 13:33
j 1Fa 14:16
k 1Fa 14:10
1Fa 15:29
l 1Fa 14:11
Ayu 21:19
m 1Fa 14:19
1Fa 15:31
n 1Fa 15:21
1Fa 15:33
o Kut 20:5
Kut 34:7
p 1Fa 16:13
q Zb 115:4
Isa 2:8
Isa 44:9
r 1Fa 14:14
1Fa 15:27

Safu ya 2

a 2Fa 9:31
b Met 20:1
Met 31:4
Lu 21:34
c Mwa 24:2
Mwa 39:4
d 2Fa 9:31
e 1Sa 25:22
1Fa 14:10
2Fa 9:8
f Hes 35:19
Hes 35:31
g Zb 9:5
Zb 109:13
h 1Fa 16:3
i 1Fa 16:1
j 1Fa 16:6
k Kum 32:21
1Sa 12:21
2Fa 17:15
Isa 41:29
Yer 10:14
Mdo 14:15
Ro 1:23
1Ko 8:4
1Ko 10:19
l 1Fa 14:19
m Ayu 20:5
n Yos 19:44
Yos 21:23
1Fa 15:27

wakamfanya Omri,[a] mkuu wa
jeshi, kuwa mfalme juu ya
Israeli siku hiyo katika ka-
mbi. **17** Sasa Omri na Israe-
li wote pamoja naye wakapa-
nda kutoka Gibethoni, waka-
anza kuzingira[b] Tirsa. **18** Na
ikawa kwamba mara tu Zimri
alipoona kwamba jiji limete-
kwa, akaingia katika mnara wa
makao wa nyumba ya mfalme,
akaiteketeza kwa moto nyu-
mba ya mfalme juu yake mwe-
nyewe, hivi kwamba akafa,[c]
19 kwa ajili ya dhambi zake ali-
zotenda kwa kufanya yaliyoku-
wa mabaya machoni pa Yeho-
va[d] kwa kutembea katika njia
ya Yeroboamu na katika dha-
mbi yake aliyotenda kwa ku-
sababisha Israeli watende dha-
mbi.[e] **20** Na mambo mengine
ya Zimri na hila yake aliyopa-
nga, je, hayakuandikwa katika
kitabu[f] cha mambo ya siku za
wafalme wa Israeli?

21 Wakati huo ndipo watu
wa Israeli walianza kujigawa-
nya kuwa sehemu mbili.[g]
Kuna sehemu moja ya watu
waliokuwa wafuasi wa Tibni
mwana wa Ginathi, ili kumfa-
nya kuwa mfalme, na sehemu
ile nyingine wafuasi wa Omri.
22 Mwishowe watu waliokuwa
wakimfuata Omri wakawashi-
nda watu waliokuwa wakimfu-
ata Tibni mwana wa Ginathi;
kwa hiyo Tibni akafa, na Omri
akaanza kutawala.

23 Katika mwaka wa 31 wa
Asa mfalme wa Yuda, Omri aka-
wa mfalme juu ya Israeli kwa
miaka 12. Akatawala miaka 6
kule Tirsa. **24** Naye akanu-
nua mlima wa Samaria kutoka
kwa Shemeri kwa talanta mbi-
li za fedha, naye akaanza kuje-
nga juu ya huo mlima na kuita
jina la jiji alilolijenga Samaria,[h]

SURA 16

a 2Fa 8:26
Met 28:2
Mik 6:16
b Kum 20:19
c Amu 9:54
1Sa 31:4
2Sa 17:23
Mt 27:5
d 1Fa 15:30
Zb 9:16
e 1Fa 12:28
1Fa 14:9
f 1Fa 14:19
1Fa 15:31
1Fa 16:5
1Fa 22:39
g Met 28:2
Mt 12:25
h 1Fa 20:1
1Fa 22:37
2Fa 17:24
Amo 6:1
Mdo 8:5

Safu ya 2

a 1Fa 14:9
Mik 6:16
b 1Fa 12:28
1Fa 13:33
c 1Fa 16:13
d 1Fa 14:19
e 1Fa 16:33
1Fa 21:4
1Fa 21:21
2Fa 10:1
2Nya 18:1
f 1Fa 16:24
1Fa 20:10
Isa 7:9
g 1Fa 16:25
1Fa 21:25
2Fa 3:2
h Sef 3:2
i 1Fa 12:28
j 1Fa 18:4
1Fa 18:19
1Fa 19:1
1Fa 21:7
1Fa 21:25
2Fa 9:30
Ufu 2:20
k Mwa 10:15
1Fa 11:1
l Kum 7:3
Yos 23:12
m Amu 2:11
Amu 10:6
2Fa 10:19
2Fa 17:16
n 2Fa 10:21
2Fa 10:27
o Kut 34:13
2Fa 10:26
2Fa 13:6
p 1Fa 14:9

kulingana na jina la Shemeri
bwana wa ule mlima. **25** Na
Omri akazidi kutenda yaliyoku-
wa mabaya machoni pa Yeho-
va, akatenda yaliyokuwa maba-
ya zaidi kuliko wote waliomta-
ngulia.[a] **26** Naye akatembea
katika njia yote ya Yeroboamu
mwana wa Nebati[b] na katika
dhambi yake ambayo kupitia
hiyo alisababisha Israeli kute-
nda dhambi kwa kumtia uchu-
ngu Yehova Mungu wa Israe-
li, kwa sanamu zao za ubati-
li.[c] **27** Na mambo mengine ya
Omri, yale aliyoyafanya na ngu-
vu zake alizotumia kutenda, je,
hayakuandikwa katika kitabu[d]
cha mambo ya siku za wafa-
lme wa Israeli? **28** Mwishowe
Omri akalala pamoja na maba-
bu zake, akazikwa Samaria; na
Ahabu[e] mwana wake akaanza
kutawala mahali pake.

29 Naye Ahabu mwana wa
Omri alikuwa mfalme juu ya
Israeli katika mwaka wa 38
wa Asa mfalme wa Yuda; na
Ahabu mwana wa Omri akae-
ndelea kutawala juu ya Isra-
eli katika Samaria[f] kwa mia-
ka 22. **30** Na Ahabu mwana
wa Omri akatenda mabaya zai-
di machoni pa Yehova kuliko
wote waliomtangulia.[g] **31** Na
ikawa kana kwamba lilikuwa ni
jambo dogo zaidi[h] kwake kute-
mbea katika dhambi za Yero-
boamu[i] mwana wa Nebati, sasa
akamchukua Yezebeli[j] binti ya
Ethbaali, mfalme wa Wasidoni,[k]
kuwa mke wake[l] naye akaanza
kwenda kumtumikia Baali[m] na
kumwinamia. **32** Tena aka-
msimamishia Baali madhabahu
katika nyumba[n] ya Baali ali-
yoijenga kule Samaria. **33** Na
Ahabu akatengeneza mti mta-
katifu;[o] na Ahabu akafanya me-
ngi zaidi ya kumtia uchungu[p]

Yehova Mungu wa Israeli, kuliko wafalme wote wa Israeli waliomtangulia.

34 Katika siku zake Hieli Mbetheli akajenga Yeriko. Kwa kufiwa na Abiramu mzaliwa wake wa kwanza yeye aliuweka msingi wake, na kwa kufiwa na Segubu mwana wake aliye mdogo zaidi yeye aliisimamisha milango yake, kulingana na neno la Yehova alilosema kupitia Yoshua mwana wa Nuni.[a]

17 Na Eliya[b] Mtishbi kutoka kwa wakaaji wa Gileadi[c] akamwambia Ahabu: "Kama anavyoishi[d] Yehova Mungu wa Israeli, ambaye ninasimama mbele zake,[e] miaka hii hakutakuwa na umande wala mvua,[f] isipokuwa kwa agizo la neno langu!"[g]

2 Basi neno[h] la Yehova likamjia, na kusema: **3** "Ondoka hapa, ugeuke, ushike njia kwenda upande wa mashariki, ujifiche[i] kwenye bonde la mto la Kerithi lililoko mashariki mwa Yordani. **4** Na itatukia kwamba unapaswa kunywa[j] kutoka katika hilo bonde la mto, nami nitawaamuru kunguru[k] wakuletee chakula huko."[l] **5** Naye akaenda mara moja na kufanya kulingana na neno la Yehova,[m] na kwa hiyo akaenda, akaanza kukaa kando ya lile bonde la mto la Kerithi lililoko mashariki mwa Yordani. **6** Na kunguru wakamletea mkate na nyama wakati wa asubuhi na mkate na nyama wakati wa jioni, naye akaendelea kunywa maji katika lile bonde la mto.[n] **7** Lakini ikawa kwamba baada ya siku kadhaa, lile bonde la mto likakauka,[o] kwa sababu mvua haikuwa imenyesha juu ya dunia.

8 Basi neno la Yehova likamjia, na kusema:[a] **9** "Ondoka, nenda Sarefathi,[b] wa Sidoni, nawe ukae huko. Tazama! Nitamwamuru mwanamke fulani huko, mjane, akupe chakula." **10** Basi akaondoka, akaenda Sarefathi, akafika kwenye mwingilio wa jiji; na tazama! mwanamke, mjane, alikuwa hapo akikusanya kuni. Basi akamwita na kumwambia yule mwanamke: "Tafadhali, niletee maji kidogo katika chombo ninywe."[c] **11** Mwanamke huyo alipoanza kwenda kuyaleta, akamwita na kumwambia: "Tafadhali, niletee kipande cha mkate[d] mkononi mwako." **12** Ndipo mwanamke yule akasema: "Kama anavyoishi Yehova Mungu wako,[e] mimi sina keki yoyote ya mviringo,[f] isipokuwa mkono mmoja tu[g] wa unga katika mtungi mkubwa na mafuta kidogo[h] katika mtungi mdogo; na tazama, ninakusanya kuni chache, nami nitaenda kutayarisha kitu kwa ajili yangu na mwanangu, nasi tutakula chakula hicho na kufa."[i]

13 Ndipo Eliya akamwambia: "Usiogope.[j] Nenda, fanya kulingana na neno lako. Ila tu unitayarishie kwanza keki ndogo ya mviringo kutokana na kile kilichopo,[k] nawe uniletee hiyo, na unaweza kutayarisha kitu kwa ajili yako na mwana wako baadaye. **14** Kwa maana Yehova Mungu wa Israeli, amesema hivi, 'Ule mtungi mkubwa wa unga hautamalizika, na ule mtungi mdogo wa mafuta hautapungua mpaka siku Yehova atakapoleta mvua juu ya uso wa nchi.'"[l] **15** Basi akaenda na kufanya kulingana na neno la Eliya; na mwanamke yule akaendelea kula, yeye

SURA 16
a Yos 6:26
Yos 23:14
Zek 1:6

SURA 17
b 1Fa 17:16
1Fa 17:22
1Fa 18:36
1Fa 18:46
2Fa 2:8
2Fa 2:11
2Nya 21:12
Lu 1:17
Yoh 1:21
c Yos 22:9
2Fa 10:33
d Kum 6:13
1Sa 19:6
1Fa 22:14
2Fa 3:14
Yer 12:16
e Kum 10:8
Lu 1:19
f Law 26:21
Kum 28:23
g Yer 14:22
Lu 4:25
Yak 5:17
h Hes 12:6
i Zb 31:20
Zb 83:3
j Zb 110:7
k Zb 147:9
Ro 8:28
l Zb 37:5
Zb 37:25
Mt 6:11
2Pe 2:9
m Zb 119:60
Met 3:5
n Hes 11:23
Amu 15:19
Zb 37:19
o 1Fa 18:5
Ayu 6:15

Safu ya 2
a Zb 36:10
b Oba 20
Lu 4:26
c Mwa 24:17
Mt 10:42
Yoh 4:7
Ebr 11:37
d Mwa 18:5
e Kum 6:13
Yer 4:2
f Mwa 18:6
g Mt 15:33
h 2Fa 4:2
i Omb 4:9
j Isa 41:10
k Met 3:9
Mt 19:21
1Pe 1:7
l Zb 34:10
Met 3:10
Flp 4:19

pamoja na Eliya na nyumba ya
yule mwanamke, kwa siku nyi-
ngi.[a] **16** Ule mtungi mkubwa
wa unga haukumalizika, wala
ule mtungi mdogo wa mafu-
ta haukupungua,[b] kulingana na
neno la Yehova alilokuwa ame-
sema kupitia Eliya.

17 Na ikawa kwamba baada
ya mambo hayo mwana wa
yule mwanamke, bimkubwa wa
ile nyumba, akawa mgonjwa,
na ugonjwa wake ukawa mka-
li sana hivi kwamba hapakuwa
na pumzi iliyobaki ndani yake.[c]
18 Ndipo akamwambia Eliya:
"Nina nini nawe,[d] Ee mtu wa
Mungu wa kweli? Umekuja kwa-
ngu ili kurudisha kumbukumbu
la kosa langu[e] na kumuua mwa-
nangu." **19** Lakini akamwa-
mbia: "Nipe mwana wako." Ki-
sha akamchukua kutoka ki-
fuani pake, akampeleka juu
katika chumba cha darini,[f] ali-
pokuwa akikaa, akamlaza juu
ya kitanda chake mwenyewe.[g]
20 Naye akaanza kumwita Ye-
hova na kusema: "Ee Yehova
Mungu wangu,[h] je, tena unale-
ta mabaya juu ya mjane nina-
yekaa naye kwa kumuua mwa-
na wake?" **21** Naye akajinyoo-
sha juu ya yule mtoto[i] mara tatu
na kumwita Yehova na kusema:
"Ee Yehova, Mungu wangu, ta-
fadhali, irudishe nafsi[j] ya mto-
to huyu ndani yake." **22** Mwi-
showe Yehova akaisikiliza sau-
ti ya Eliya,[k] hivi kwamba nafsi
ya yule mtoto ikarudi ndani
yake, akawa hai.[l] **23** Basi Eli-
ya akamchukua mtoto huyo,
akamshusha kutoka katika
kile chumba cha darini, aka-
mleta katika nyumba na ku-
mpa mama yake; na kisha
Eliya akasema: "Tazama, mwa-
na wako yuko hai."[m] **24** Ndipo
yule mwanamke akamwambia
Eliya: "Kwa kweli sasa najua
kwamba wewe ni mtu wa Mu-
ngu[a] na kwamba neno la Yehova
kinywani mwako ni la kweli."[b]

18 Na ikawa kwamba baa-
da ya siku nyingi neno
la Yehova likamjia Eliya katika
mwaka wa tatu, na kusema:
"Nenda, jionyeshe kwa Ahabu,
kwa kuwa nimeazimia kunye-
sha mvua[c] juu ya uso wa nchi."[d]
2 Basi Eliya akaenda kujionye-
sha kwa Ahabu, njaa ilipokuwa
kali[e] katika Samaria.

3 Wakati huo Ahabu aka-
mwita Obadia, aliyekuwa akii-
simamia nyumba.[f] (Basi Obadia
alikuwa amejionyesha kuwa
mtu anayemwogopa[g] Yehova
sana. **4** Na ikawa kwamba Ye-
zebeli[h] alipowakatilia mbali ma-
nabii[i] wa Yehova, Obadia aliwa-
chukua manabii 100, akawafi-
cha wakiwa vikundi viwili vya
watu 50 pangoni, naye akawapa
mkate na maji.)[j] **5** Na Ahabu
akamwambia Obadia: "Tembea
katika nchi kwenye mabubuji-
ko yote ya maji na kwenye ma-
bonde yote ya mito. Labda tuta-
pata majani mabichi,[k] ili tuwa-
hifadhi hai farasi na nyumbu
na ili wanyama zaidi wasianga-
mie."[l] **6** Kwa hiyo wakagawa-
na nchi ambayo wangepita kati-
kati yake. Ahabu akaenda peke
yake kupitia njia moja, na Oba-
dia akaenda peke yake kupitia
njia nyingine.[m]

7 Obadia alipoendelea kusa-
firi njiani, tazama, Eliya aki-
ja kumpokea.[n] Mara moja aka-
mtambua, akaanguka kifudifu-
di,[o] akasema: "Je, ni wewe, bwa-
na wangu[p] Eliya?" **8** Naye
akamwambia: "Ni mimi. Nenda,
mwambie bwana wako,[q] 'Taza-
ma, Eliya yupo hapa.'" **9** La-
kini akasema: "Nimetenda dha-

SURA 17
a 2Nya 20:20; Mt 10:41; Lu 4:25
b Zb 37:19; Met 11:24; Lu 18:27; 2Ko 9:10
c Mwa 2:7; 2Fa 4:20; Ayu 34:14; Mhu 9:11
d 2Sa 16:10; 2Sa 19:22; 2Fa 3:13; Mt 8:29; Mk 1:24; Yoh 2:4
e Ayu 13:26
f 2Fa 4:10; Mdo 9:37
g 2Fa 4:21; 2Fa 4:32
h 1Fa 18:36; Zb 99:6; Mt 21:22
i 2Fa 4:34; Mdo 20:10
j Mwa 35:18; Yer 15:9
k Zb 65:2; Met 15:8; Mdo 9:40; Ebr 11:19; Yak 5:16
l Kum 32:39; 1Sa 2:6; 2Fa 4:34; 2Fa 13:21; Lu 7:15; Lu 8:55; Yoh 5:28; Yoh 11:44; Mdo 9:41; Mdo 20:10; Ro 14:9
m Ebr 11:35

Safu ya 2
a Yoh 3:2
b 1Th 2:13; 1Yo 2:21

SURA 18
c Lu 4:25; Yak 5:17
d Zb 65:9; Zb 65:10; Yer 14:22; Mt 5:45
e Law 26:26; Kum 28:24; Omb 4:9
f Mwa 24:2; Mwa 39:4
g Met 8:13; Met 14:26; Mal 3:16; Mdo 10:2
h 1Fa 16:31
i Ne 9:26; Zb 105:15
j Met 19:17; Mt 10:42
k Zb 104:14
l Yer 14:5; Yoe 1:18
m Yer 14:3
n 2Fa 1:8
o 1Sa 25:23
p 2Fa 8:12
q 1Pe 2:17

mbi gani[a] ndipo umtie mtumishi wako mkononi mwa Ahabu, aniue? **10** Kama anavyoishi Yehova Mungu wako,[b] hakuna taifa wala ufalme ambapo bwana wangu hajawatuma watu wakutafute. Waliposema, 'Hayupo hapa,' akafanya ufalme na taifa kuapa kwamba hawakuweza kukupata.[c] **11** Na sasa unasema, 'Nenda, mwambie bwana wako: "Tazama, Eliya yupo hapa."' **12** Na hakika itatukia kwamba, mimi nikiondoka kwako, ndipo roho[d] ya Yehova itakapokuchukua na kukupeleka mahali ambapo mimi sitajua; nami nitakuwa nimekuja kumwambia Ahabu, naye hatakupata, naye hakika ataniua,[e] kwa kuwa mtumishi wako amemwogopa Yehova tangu ujana wake.[f] **13** Je, bwana wangu hakuambiwa yale niliyofanya wakati Yezebeli alipowaua manabii wa Yehova, jinsi nilivyowaficha baadhi ya manabii wa Yehova, watu 100 wakiwa vikundi viwili vya watu 50 pangoni,[g] nikaendelea kuwapa mkate na maji?[h] **14** Na sasa unasema, 'Nenda, mwambie bwana wako: "Tazama, Eliya yupo hapa."' Naye hakika ataniua."[i] **15** Hata hivyo, Eliya akasema: "Kama anavyoishi[j] Yehova wa majeshi[k] ambaye ninasimama mbele zake, leo nitajionyesha kwake."

16 Basi Obadia akaenda kukutana na Ahabu, akamwambia; na kwa hiyo Ahabu akaenda kukutana na Eliya.

17 Na ikawa kwamba, mara tu Ahabu alipomwona Eliya, mara moja Ahabu akamwambia: "Je, ni wewe, mtu unayeleta taabu juu ya Israeli?"[l]

18 Naye akasema: "Mimi sikuleta taabu juu ya Israeli,[m] lakini ni wewe na nyumba ya baba yako,[a] kwa sababu ninyi mmeziacha amri za Yehova,[b] nawe ukaanza kufuata Mabaali.[c] **19** Na sasa tuma watu, unikusanyie Israeli wote katika Mlima Karmeli[d] na pia wale manabii 450 wa Baali[e] na wale manabii 400 wa ule mti mtakatifu,[f] wanaokula mezani pa Yezebeli."[g] **20** Na Ahabu akatuma watu kati ya wana wote wa Israeli, akawakusanya wale manabii[h] katika Mlima Karmeli.

21 Kisha Eliya akawakaribia watu wote na kusema: "Mtayumba-yumba juu ya maoni mawili tofauti mpaka wakati gani?[i] Ikiwa Yehova ndiye Mungu wa kweli, mfuateni yeye;[j] lakini ikiwa ni Baali, mfuateni yeye." Na watu hawakumjibu neno lolote. **22** Na Eliya akaendelea kuwaambia watu: "Mimi tu nimebaki nikiwa nabii wa Yehova,[k] mimi peke yangu, nao manabii wa Baali ni watu 450. **23** Sasa na watupe sisi ng'ombe-dume wachanga wawili, nao wajichagulie ng'ombe-dume mmoja mchanga, wamkate vipande-vipande na kumweka juu ya kuni, lakini wasiziwashe moto. Na mimi nitamtayarisha yule ng'ombe mchanga mwingine, nami nitamweka juu ya kuni, lakini sitaziwasha moto. **24** Nanyi mliitie jina la mungu wenu,[l] nami, kwa upande wangu, nitaliitia jina la Yehova; na itatukia kwamba yule Mungu wa kweli atakayejibu kupitia moto,[m] huyo ndiye Mungu wa kweli."[n] Kwa hiyo watu wote wakajibu na kusema: "Jambo hili ni jema."

25 Sasa Eliya akawaambia manabii wa Baali: "Jichagulieni ng'ombe mchanga mmoja, halafu mkamtayarishe kwanza,

SURA 18
a 1Fa 17:18
b Kum 6:13
1Fa 1:29
c 1Fa 17:3
1Fa 17:9
d 2Fa 2:16
Eze 3:12
Mt 4:1
Mdo 8:39
e Met 16:14
f Zb 18:21
Zb 71:17
Met 8:13
Mhu 7:18
Mhu 12:1
Isa 50:10
g 1Fa 18:4
h Mt 25:35
i Met 22:3
j Kum 6:13
Isa 49:18
k 1Sa 4:4
Zb 24:10
l Mdo 24:13
2Pe 2:10
Yud 8
m Yos 7:25

Safu ya 2
a Eze 3:8
b Kut 20:4
1Fa 9:9
Yer 2:13
c 1Fa 16:31
d Yos 19:26
2Fa 2:25
Yer 46:18
Amo 1:2
e Eze 13:3
f 1Fa 16:33
g 1Fa 19:1
h 1Fa 22:6
i Kum 4:35
2Fa 17:41
Isa 42:8
Yer 2:11
Ho 10:2
Mt 12:30
1Ko 10:21
2Ko 6:14
j Kut 20:5
Yos 24:15
1Sa 7:3
Zb 100:3
k 1Fa 19:10
l Amu 6:31
m Kum 4:24
n Law 9:24
Amu 6:21
1Nya 21:26
2Nya 7:1

kwa sababu ninyi ndio wengi;
nanyi mliitie jina la mungu
wenu, lakini msiwashe moto.”
26 Basi wakamchukua yule
ng’ombe mchanga aliyewapa.
Kisha wakamtayarisha, nao
wakaendelea kuliitia jina la Ba-
ali kutoka asubuhi mpaka kati-
kati ya mchana, wakisema: “Ee
Baali, tupe jibu!” Lakini hapa-
kuwa na sauti yoyote,[a] wala ha-
kuna yeyote aliyetoa jibu.[b] Nao
wakazidi kurukaruka kuizu-
nguka madhabahu waliyokuwa
wameitengeneza. **27** Na ika-
wa kwamba ilipofika katikati
ya mchana Eliya akaanza ku-
wafanyia dhihaka[c] na kusema:
“Iteni kwa sauti kubwa, kwa
maana yeye ni mungu;[d] kwa
maana lazima iwe ana kazi fu-
lani, naye ana kinyesi[e] na lazi-
ma aende chooni.[f] Au pengi-
ne amelala usingizi naye anapa-
swa kuamka!”[g] **28** Nao waka-
anza kuita kwa sauti yao
yote, wakijikatakata[h] kwa visu
na mikuki kulingana na de-
sturi yao, mpaka walipojitiriri-
sha damu. **29** Na ikawa kwa-
mba mara tu mchana ulipo-
kwisha nao wakazidi kutenda
kama manabii[i] mpaka wakati
wa kutolewa kwa toleo la nafa-
ka, hapakuwa na sauti yoyote,
wala hapakuwa na yeyote aliye-
jibu, wala aliyewasikiliza.[j]
30 Mwishowe Eliya akawaam-
bia watu wote: “Nikaribie-
ni.” Basi watu wote wakamka-
ribia. Kisha akatengeneza ile
madhabahu ya Yehova iliyoku-
wa imebomoka.[k] **31** Basi Eli-
ya akachukua mawe kumi na
mawili, kulingana na hesabu
ya makabila ya wana wa Ya-
kobo, ambaye neno la Yeho-
va lilikuwa limemjia,[l] likisema:
“Jina lako litakuwa Israeli.”[m]
32 Naye akafanyiza mawe ya-

SURA 18

a Zb 115:7
b Zb 115:5
Zb 135:16
Isa 44:18
Isa 45:20
Yer 10:5
Da 5:23
Hab 2:18
1Ko 8:4
1Ko 10:19
1Ko 12:2
c Yer 10:15
d Isa 41:23
e Mt 15:17
f Amu 3:24
1Sa 24:3
g Zb 121:4
Zb 135:17
Isa 40:28
h Law 19:28
Kum 14:1
i 1Sa 18:10
1Fa 22:10
j Isa 44:20
Ga 4:8
k 1Fa 19:14
l Kut 24:4
Yos 4:3
m Mwa 32:28
Mwa 33:20
Mwa 35:10
2Fa 17:34
Isa 48:1

Safu ya 2

a Kut 20:25
Kum 27:6
b Mwa 13:18
Kum 12:27
1Fa 18:24
c Mwa 22:9
Law 1:7
d Kut 29:41
Zb 141:2
Mdo 3:1
e Mwa 26:24
2Nya 20:7
f Mwa 28:13
Mwa 31:53
Mwa 32:9
Mwa 46:3
g 1Nya 29:18
Mt 22:32
h Kut 20:2
Zb 83:18
Eze 36:23
i Hes 16:28
2Sa 7:21
Yoh 11:42
j 2Nya 14:11
Zb 96:5
Isa 44:6
Da 4:37
k Yer 31:18
Eze 18:32
Eze 33:11
l Law 9:24
Amu 6:21
2Nya 7:1
m 1Fa 18:23
n 1Fa 18:24
o 2Nya 7:3
Yak 4:10

kawa madhabahu[a] kwa jina la
Yehova,[b] akachimba mtaro we-
nye ukubwa wa kama sehemu
inayopandwa vipimo viwili vya
sea vya mbegu, kuizunguka
madhabahu yote. **33** Kisha
akapanga kwa utaratibu zile
kuni,[c] akamkata yule ng’ombe
mchanga vipande-vipande na
kumweka juu ya zile kuni. Sasa
akasema: “Jazeni maji mitungi
mikubwa minne, myamwage
juu ya toleo la kuteketezwa na
juu ya kuni.” **34** Kisha akase-
ma: “Fanyeni hivyo tena.” Basi
wakafanya hivyo tena. Lakini
akasema: “Fanyeni hivyo mara
ya tatu.” Basi wakafanya hivyo
mara ya tatu. **35** Kwa hiyo
maji yakaizunguka ile madha-
bahu yote, na pia ule mtaro aka-
ujaza maji.
36 Na ikawa kwamba wa-
kati[d] wa kutolewa kwa toleo
la nafaka, Eliya nabii akaa-
nza kukaribia na kusema: “Ee
Yehova Mungu wa Abrahamu,[e]
Isaka[f] na Israeli,[g] leo na iju-
likane kwamba wewe ni Mu-
ngu katika Israeli[h] na mimi ni
mtumishi wako na ni kwa neno[i]
lako nimefanya mambo haya
yote. **37** Unijibu, Ee Yehova,
unijibu, ili watu hawa wajue
kwamba wewe, Yehova,[j] ndiye
Mungu wa kweli na wewe mwe-
nyewe umeugeuza moyo wao
urudi.”[k]
38 Ndipo moto[l] wa Yehova
ukashuka, ukala lile toleo la ku-
teketezwa[m] na zile kuni na
mawe na mavumbi, nao uka-
ramba maji yaliyokuwa kati-
ka mtaro.[n] **39** Watu wote wa-
lipoona jambo lile, wakaanguka
kifudifudi[o] mara moja, na ku-
sema: “Yehova ndiye Mungu
wa kweli! Yehova ndiye Mu-
ngu wa kweli!” **40** Kisha Eli-

ya akawaambia: “Wakamateni manabii wa Baali! Msiache hata mmoja wao aponyoke!” Ndipo wakawakamata mara moja, na Eliya akawashusha mpaka kwenye bonde la mto la Kishoni,[a] akawaua huko.[b]

41 Sasa Eliya akamwambia Ahabu: “Panda ukale na kunywa;[c] kwa maana kuna kishindo cha machafuko ya mvua kubwa.”[d] **42** Na Ahabu akapanda, akaenda zake kula na kunywa. Naye Eliya akapanda juu ya Karmeli na kuanza kuchutama chini,[e] akaweka uso wake katikati ya magoti yake.[f] **43** Kisha akamwambia mtumishi wake: “Nenda juu, tafadhali. Tazama upande wa bahari.” Basi akaenda juu, akatazama na kisha akasema: “Hakuna kitu chochote.” Naye akaendelea kusema, “Rudi,” mara saba.[g] **44** Na ikawa kwamba mara ya saba akasema: “Tazama! Pana wingu dogo kama kiganja cha mkono wa mwanadamu linalopanda kutoka baharini.”[h] Sasa akasema: “Nenda juu, mwambie Ahabu, ‘Funga gari![i] Nawe ushuke ili mvua kubwa isikuzuie!’” **45** Na ikawa kwamba wakati huo mbingu zikatiwa giza kwa mawingu na upepo[j] na mvua kubwa sana ikaanza kunyesha.[k] Na Ahabu akaendelea kupanda gari, akaenda zake Yezreeli.[l] **46** Na mkono wa Yehova ukawa juu ya Eliya,[m] hivi kwamba akajifunga viuno,[n] naye akakimbia mbele ya Ahabu mpaka Yezreeli.[o]

19 Kisha Ahabu[p] akamwambia Yezebeli[q] mambo yote ambayo Eliya alikuwa amefanya na mambo yote kuhusu namna alivyowaua manabii wote kwa upanga.[r] **2** Ndipo Yezebeli akatuma mjumbe kwa Eliya, akisema: “Miungu na ifanye hivyo,[a] nayo izidishe jambo hilo,[b] ikiwa wakati kama huu hapo kesho sitaifanya nafsi yako iwe kama nafsi ya kila mmoja wao!” **3** Naye akaogopa. Basi akaondoka, akaanza kwenda kwa ajili ya nafsi yake,[c] akafika Beer-sheba,[d] jiji la Yuda.[e] Kisha akamwacha mtumishi wake huko. **4** Naye mwenyewe akaingia nyikani safari ya siku moja, mwishowe akafika na kuketi chini ya mretemu fulani.[f] Naye akaanza kuomba kwamba nafsi yake ife na kusema: “Inatosha! Sasa, Ee Yehova, iondoe nafsi yangu,[g] kwa maana mimi si bora kuliko mababu zangu.”

5 Mwishowe akalala chini, akashikwa na usingizi chini ya ule mretemu.[h] Lakini, tazama! Malaika[i] akamgusa.[j] Ndipo akamwambia: “Amka, ule.” **6** Alipoangalia, na tazama, pale karibu na kichwa chake palikuwa na keki ya mviringo[k] juu ya mawe yenye moto na gudulia la maji. Naye akaanza kula na kunywa, kisha akalala chini tena. **7** Baadaye yule malaika[l] wa Yehova akarudi mara ya pili, akamgusa na kusema: “Amka, ule, kwa maana safari ni ndefu mno kwako.”[m] **8** Basi akaamka, akala na kunywa, naye akazidi kwenda katika nguvu za chakula kile kwa siku 40,[n] mchana na usiku, mpaka Horebu, mlima wa Mungu wa kweli.[o]

9 Mwishowe hapo akaingia pangoni,[p] ili alale humo usiku; na tazama! palikuwa na neno la Yehova kwa ajili yake, nalo likamwambia: “Una kazi gani hapa, Eliya?”[q] **10** Naye akasema: “Nimekuwa na wivu[r]

SURA 18
a Amu 5:21; Zb 83:9
b Kum 13:5; Kum 18:20
c Mhu 9:7
d 1Fa 17:1; Zek 10:1
e Yos 7:6; Yak 5:16
f Zb 89:7; Ebr 12:28; Yak 5:17
g Lu 18:7
h Lu 12:54
i Mik 1:13
j Zb 107:25; Zb 147:18; Yak 5:18
k 1Sa 12:18; Ayu 38:37; Zb 68:9
l Yos 19:18; 1Fa 21:1
m Isa 8:11; Eze 3:14
n Kut 12:11; 2Fa 4:29; 2Fa 9:1; 1Pe 1:13
o 1Sa 8:11; 1Pe 2:17

SURA 19
p 1Fa 16:29; 1Fa 21:25
q 1Fa 16:31
r 1Fa 18:40

Safu ya 2
a 1Fa 20:10
b Mdo 23:13
c Kut 2:15; 1Sa 27:1; Met 16:14; Met 22:3; Mt 10:23
d Mwa 21:31
e Yos 15:28
f Yon 4:6
g Hes 11:15; Ayu 3:21; Yon 4:3
h Ayu 30:4
i Zb 34:7
j Da 10:10; Mdo 12:7
k 1Fa 17:12; Isa 33:16
l Ebr 1:14
m Zb 103:13
n Kut 24:18; Kum 9:9; Lu 4:2
o Kut 3:1; Kut 19:18; Mal 4:4
p Kut 33:22; Ebr 11:38
q Mwa 16:8; Zb 139:7
r Kut 20:5; Hes 25:11; 2Fa 10:16; Zb 69:9; Zb 119:139; 2Ko 11:2

kwelikweli kwa ajili ya Yehova Mungu wa majeshi; kwa maana wana wa Israeli wameliacha agano lako,[a] wamezibomoa[b] madhabahu zako, nao wamewaua manabii wako kwa upanga,[c] hivi kwamba ni mimi peke yangu nimebaki;[d] nao wanaanza kuitafuta nafsi yangu ili kuiondoa."[e] **11** Lakini likasema: "Toka, usimame juu ya mlima mbele za Yehova."[f] Na tazama! Yehova alikuwa anapita karibu,[g] na upepo mkubwa na wenye nguvu ukawa unapasua milima na kuvunja miamba mbele za Yehova.[h] (Yehova hakuwa katika upepo ule.) Na baada ya upepo ule kukawa na tetemeko.[i] (Yehova hakuwa katika lile tetemeko.) **12** Na baada ya lile tetemeko kukawa na moto.[j] (Yehova hakuwa katika moto ule.) Na baada ya moto ule kukawa na sauti tulivu, ya chini.[k] **13** Na ikawa kwamba mara tu Eliya alipoisikia, akafunika uso wake mara moja katika vazi lake rasmi,[l] akatoka nje, akasimama mlangoni pa lile pango; na tazama! palikuwa na sauti kwa ajili yake, nayo ikamwambia: "Una kazi gani hapa, Eliya?"[m] **14** Naye akasema: "Nimekuwa na wivu kwelikweli kwa ajili ya Yehova Mungu wa majeshi; kwa maana wana wa Israeli wameliacha agano lako,[n] wamezibomoa madhabahu zako, nao wamewaua manabii wako kwa upanga, hivi kwamba ni mimi peke yangu nimebaki; nao wanaanza kuitafuta nafsi yangu ili kuiondoa."[o]

15 Sasa Yehova akamwambia: "Nenda, rudi katika nyika ya Damasko;[p] nawe uingie na kumtia mafuta[q] Hazaeli[r] kuwa mfalme juu ya Siria. **16** Na Yehu[a] mjukuu wa Nimshi[b] umtie mafuta kuwa mfalme juu ya Israeli; na Elisha[c] mwana wa Shafati kutoka Abel-mehola[d] umtie mafuta kuwa nabii mahali pako.[e] **17** Na itatukia kwamba yule atakayepona upanga[f] wa Hazaeli, Yehu atamuua;[g] na yule atakayepona upanga wa Yehu, Elisha atamuua.[h] **18** Nami nimewaacha watu elfu saba wabaki katika Israeli,[i] magoti yote ambayo hayakumwinamia Baali,[j] na kila kinywa ambacho hakikumbusu."[k]

19 Basi akaondoka hapo, akamkuta Elisha mwana wa Shafati akilima[l] na jozi kumi na mbili za wanyama mbele yake, naye akiwa na ile ya kumi na mbili. Basi Eliya akavuka mpaka pale alipokuwa, akalitupa vazi lake rasmi[m] juu yake. **20** Ndipo akawaacha wale ng'ombe, akakimbia kumfuata Eliya na kusema: "Tafadhali, acha nimbusu baba yangu na mama yangu.[n] Kisha nitakufuata." Naye akamwambia: "Nenda, rudi; kwa maana mimi nimekufanyia nini?" **21** Kwa hiyo akarudi, akaacha kumfuata na kisha akachukua jozi moja ya wale ng'ombe na kuwatoa dhabihu,[o] na kwa kutumia vifaa[p] vya wale ng'ombe, akatokosa nyama yao, akawapa watu, nao wakaanza kula. Kisha akaondoka, akaanza kumfuata Eliya, naye akaanza kumhudumia.[q]

20 Naye Ben-hadadi[r] mfalme wa Siria akakusanya majeshi yake yote na pia wafalme 32 pamoja naye[s] na farasi[t] na magari,[u] akapanda kwenda kuzingira[v] Samaria[w] na kupigana nalo. **2** Ki-

SURA 19
a Kum 29:25; Amu 2:20; 1Fa 8:9; 2Fa 17:15; Ebr 8:9
b Ro 11:3
c 1Fa 18:4
d 1Fa 18:22; Met 24:10; Ro 11:3
e 1Fa 19:2
f Kut 34:2
g Kut 33:22; Hab 3:3
h Ayu 38:1; Zb 50:3; Isa 29:6
i 1Sa 14:15; Ayu 9:6; Zb 68:8; Nah 1:5
j Kum 4:11
k Kut 34:6; Kum 4:33
l Kut 3:6
m 1Fa 19:9
n Kum 31:20; Zb 78:37; Isa 1:4; Yer 22:9; Ro 11:3
o 1Fa 19:10
p 2Fa 8:7
q 1Sa 2:7
r 2Fa 8:8; 2Fa 8:12; Amo 1:4

Safu ya 2
a 2Fa 9:2; 2Fa 9:30
b 2Fa 9:14
c 2Fa 2:9; Lu 4:27
d Amu 7:22; 1Fa 4:12
e 2Fa 2:15
f 2Fa 8:12; 2Fa 9:14; 2Fa 10:32; 2Fa 13:3
g 2Fa 9:24; 2Fa 10:6; 2Fa 10:25
h 2Fa 2:24
i Isa 1:9; Ro 11:4; Ro 11:5; 2Ti 2:19
j Kut 20:5
k Ho 13:2
l Kut 3:1; Amu 6:11; 2Sa 7:8
m 2Fa 2:8
n Mwa 31:28
o Law 19:5
p 2Sa 24:22
q Kut 24:13; 2Fa 2:3; 2Fa 3:11

SURA 20
r 2Fa 6:24; 2Fa 8:7
s Isa 10:8; Eze 26:7
t Met 21:31
u Kum 20:1
v Law 26:25; Kum 28:52
w 2Fa 6:24; 2Fa 17:5

sha akatuma wajumbe[a] kwa
Ahabu mfalme wa Israeli kati-
ka jiji. Naye akamwambia: "Ben-
hadadi amesema hivi, **3** 'Fe-
dha yako na dhahabu yako ni
yangu, na wake zako na wana
wako, wale wenye sura nzuri za-
idi, ni wangu.'"[b] **4** Ndipo mfa-
lme wa Israeli akajibu na kuse-
ma: "Bwana wangu mfalme, ku-
lingana na neno lako, mimi ni
wako na vyote vilivyo vyangu."[c]
5 Baadaye wajumbe waka-
rudi na kusema: "Ben-hadadi
amesema hivi, 'Nilituma watu
kwako, kusema: "Fedha yako
na dhahabu yako na wake zako
na wana wako utanipa. **6** La-
kini wakati kama huu kesho
nitawatuma watumishi wangu
kwako, nao watachunguza kwa
makini nyumba yako na nyu-
mba za watumishi wako; na
itatukia kwamba kila kitu ki-
nachotamanika[d] machoni pako
watakitia mkononi mwao, nao
watakichukua."'"
7 Kwa hiyo mfalme wa Isra-
eli akawaita wanaume wazee
wa nchi[e] na kusema: "Tafadha-
li angalieni, oneni kwamba mtu
huyu anatafuta msiba;[f] kwa
maana alituma watu kwangu
kuchukua wake zangu na wa-
nangu na fedha yangu na dha-
habu yangu, nami sikumnyi-
ma vitu hivyo." **8** Ndipo wa-
naume wazee na watu wote
wakamwambia: "Usitii, wala usi-
kubali." **9** Kwa hiyo akawaam-
bia wajumbe wa Ben-hada-
di: "Mwambieni bwana wangu
mfalme, 'Yote uliyowatuma
watu kwanza ukiyataka kwa
mtumishi wako nitafanya; laki-
ni jambo hili siwezi kulifanya.'"
Basi wale wajumbe wakaenda
zao, wakampelekea neno.
10 Sasa Ben-hadadi akatu-
ma watu kwake na kusema:

SURA 20
a 2Fa 19:9
2Fa 19:23
Isa 37:9
b Kut 15:9
Ayu 40:12
Isa 10:13
c Law 26:28
Kum 28:48
d Amu 5:30
Ezr 8:27
e Met 11:14
f Met 11:27

Safu ya 2
a 1Fa 19:2
Yer 5:7
b Mdo 23:12
c Met 16:18
Isa 37:24
d 1Sa 2:3
1Sa 25:13
Zb 45:3
e Met 27:1
Mhu 7:8
Mhu 8:7
f Met 31:4
g 1Fa 16:29
h Isa 55:11
i Kut 14:18
Zb 37:20
j 1Sa 14:6
2Nya 14:11
k Met 31:4
Mhu 10:17
Ho 4:11
l 1Fa 20:14

"Miungu[a] na inifanyie hivyo,
nayo izidishe jambo hilo,[b] iki-
wa mavumbi ya Samaria yata-
tosha mikono ya watu wote wa-
naonifuata!"[c] **11** Naye mfa-
lme wa Israeli akajibu na ku-
sema: "Mwambieni hivi, 'Mtu
anayejifunga mshipi[d] asijisifu
kama yeye anayejifungua mshi-
pi.'"[e] **12** Na ikawa kwamba
mara tu aliposikia neno hilo,
wakati yeye na wale wafalme
walipokuwa wakinywa[f] kati-
ka vibanda, mara moja akawaam-
bia watumishi wake: "Jitaya-
risheni!" Nao wakaanza kujita-
yarisha kulishambulia jiji.
13 Na tazama! nabii fulani
akamkaribia Ahabu mfalme wa
Israeli,[g] kisha akasema: "Yeho-
va amesema hivi,[h] 'Je, umeuo-
na umati huu wote mkubwa? Ta-
zama, nitautia mkononi mwako
leo, nawe hakika utajua kwa-
mba mimi ni Yehova.'"[i] **14** Ndi-
po Ahabu akasema: "Kupitia
nani?" naye akasema: "Yehova
amesema hivi, 'Kupitia vijana wa
wakuu wa wilaya za utawala.'"
Mwishowe akasema: "Ni nani
atakayeanza pambano la vita?"
naye akasema: "Ni wewe!"
15 Naye akaanza kuwahesa-
bu wale vijana wa wakuu wa
wilaya za utawala, nao wakawa
232;[j] na baada yao akawahesabu
watu wote, wana wote wa Isra-
eli, 7,000. **16** Nao wakaanza
kutoka katikati ya mchana wa-
kati Ben-hadadi alipokuwa aki-
nywa na kulewa[k] katika viba-
nda, yeye pamoja na wale wafa-
lme, wale wafalme 32 waliooku-
wa wakimsaidia. **17** Wakati
wale vijana[l] wa wakuu wa wila-
ya za utawala walipotoka kwa-
nza, mara moja Ben-hadadi
akatuma watu; nao wakaja na
kumwambia, wakisema: "Kuna
watu ambao wametoka katika

Samaria." **18** Ndipo akasema: "Hata kama wametoka kwa ajili ya amani, wakamateni wakiwa hai; au kama wametoka kwa ajili ya vita, wakamateni wakiwa hai."[a] **19** Na hao ndio waliotoka katika jiji, wale vijana wa wakuu wa wilaya za utawala na majeshi yaliyokuwa nyuma yao. **20** Nao wakaanza kumpiga na kumuua kila mmoja mtu wake; na Wasiria[b] wakaanza kukimbia,[c] na Israeli wakawafuatilia, lakini Ben-hadadi mfalme wa Siria akakimbia akiwa juu ya farasi pamoja na wapanda-farasi. **21** Lakini mfalme wa Israeli akatoka, akazidi kuwapiga na kuwaua wale farasi na magari,[d] naye akawapiga Wasiria kwa mauaji makuu.

22 Baadaye yule nabii[e] akamkaribia mfalme wa Israeli na kumwambia: "Nenda, jitie nguvu[f] na ujue na kuona utakalofanya;[g] kwa maana mwanzoni mwa mwaka mfalme wa Siria atakuja kukushambulia."[h]

23 Na watumishi wa mfalme wa Siria wakamwambia: "Mungu wao ni Mungu wa milima.[i] Ndiyo sababu walikuwa na nguvu kutushinda. Basi, na tupigane nao katika nchi tambarare, tuone kama hatutakuwa na nguvu kuwashinda. **24** Nawe ufanye hivi: Ondoa wafalme,[j] kila mmoja kutoka mahali pake, na uweke magavana mahali pao.[k] **25** Nawe ujihesabie jeshi linalolingana na jeshi lililoanguka kutoka upande wako, kukiwa na farasi kwa farasi na gari kwa gari; nasi tupigane nao katika nchi tambarare, tuone kama hatutakuwa na nguvu kuwashinda."[l] Basi akasikiliza sauti yao, akafanya vivyo hivyo.

SURA 20

a Met 16:18
Met 18:12
Lu 14:11
b Mwa 25:20
Kum 26:5
2Sa 8:6
2Fa 5:2
Isa 9:12
c Law 26:8
Kum 28:7
Zb 33:16
Zb 46:6
d Yos 11:6
e 1Fa 20:13
Amo 3:7
f 2Nya 25:8
Zb 25:8
Zb 27:14
g Met 20:18
h 2Sa 11:1
1Nya 20:1
2Nya 36:10
i Zb 47:7
Zb 83:18
Zb 97:9
Zb 115:2
Ro 1:21
1Ko 8:4
j 1Fa 20:1
1Fa 20:16
k Met 21:30
l Zb 10:3

Safu ya 2

a 1Fa 20:20
b 1Sa 29:1
2Fa 13:17
c Yos 1:11
d Amu 6:5
1Sa 13:5
2Nya 32:7
Ebr 11:34
e Zb 18:30
f Kum 32:27
Zb 58:10
Eze 20:9
Eze 36:22
g Kut 6:7
Kut 7:5
Kut 8:10
Eze 6:14
Eze 39:7
h Yos 6:15
i 1Fa 20:26
j Isa 24:18
Yer 48:44
Amo 2:14
Amo 9:3
k 1Fa 20:20
l 1Fa 22:25
m Met 20:28
Isa 16:5
n Yon 3:8
o Mwa 37:34
1Fa 21:27
Est 4:1
Isa 22:12
Ufu 11:3

26 Na ikawa kwamba mwanzoni mwa mwaka Ben-hadadi akawakusanya Wasiria[a] na kupanda mpaka Afeki[b] ili kupigana na Israeli. **27** Nao wana wa Israeli wakakusanywa na kuandaliwa,[c] wakaanza kwenda kukutana nao; na wana wa Israeli wakaenda katika kambi mbele yao kama vikundi vidogo viwili vya mbuzi, na Wasiria, kwa upande wao, wakaijaza dunia.[d] **28** Kisha yule mtu wa Mungu wa kweli[e] akakaribia na kumwambia mfalme wa Israeli, naam, akasema: "Yehova amesema hivi, 'Kwa sababu Wasiria wamesema: "Yehova ni Mungu wa milima, wala si Mungu wa nchi tambarare za chini," nitautia mkononi mwako umati huu wote mkubwa,[f] nanyi mtajua hakika kwamba mimi ni Yehova.'"[g]

29 Nao wakaendelea kukaa kambini siku saba, hawa wakiwa mbele ya wale.[h] Na ikawa kwamba katika siku ya saba lile pambano la kivita likaanza; na wana wa Israeli wakawapiga na kuwaua Wasiria, watu mia moja elfu wanaoenda kwa miguu, katika siku moja. **30** Na wale waliobaki wakakimbia mpaka Afeki,[i] katika jiji; na ukuta ukaanguka juu ya watu 27,000 waliokuwa wamebaki.[j] Naye Ben-hadadi akakimbia,[k] mwishowe akafika jijini, akaingia katika chumba cha ndani kabisa.[l]

31 Kwa hiyo watumishi wake wakamwambia: "Tazama, sasa, tumesikia kwamba wafalme wa nyumba ya Israeli ni wafalme walio na fadhili zenye upendo.[m] Tafadhali, acha tuchukue nguo za magunia[n] katika viuno[o] vyetu na kamba juu ya vichwa vyetu, nasi twende

kwa mfalme wa Israeli. Pengine atahifadhi hai nafsi yako."[a]
32 Basi wakajifunga nguo za magunia katika viuno vyao, na kamba zikiwa juu ya vichwa vyao, wakaja kwa mfalme wa Israeli na kusema: "Mtumishi wako Ben-hadadi amesema, 'Tafadhali, acha nafsi yangu iishi.'" Naye akasema: "Je, yeye angali hai bado? Yeye ni ndugu yangu." **33** Basi hao watu[b] wakaliona jambo hilo kuwa ni ishara ya bahati na bila kukawia wakaliona kuwa ni uamuzi wake mwenyewe, nao wakaendelea kusema: "Ben-hadadi ni ndugu yako." Kwa hiyo akasema: "Haya, mleteni." Ndipo Ben-hadadi akaenda kwake; naye akampandisha garini mara moja.[c]

34 Sasa Ben-hadadi akamwambia: "Majiji[d] ambayo baba yangu aliyachukua kutoka kwa baba yako nitayarudisha; nawe utajipa barabara katika Damasko kama vile baba yangu alivyojipa katika Samaria."

"Nami nitakuacha uende zako kwa agano."[e]

Kwa hiyo akafanya agano naye na kumwacha aende zake.

35 Na mtu fulani wa wana wa manabii[f] akamwambia rafiki yake kwa neno[g] la Yehova: "Tafadhali, nipige." Lakini yule mtu akakataa kumpiga. **36** Kwa hiyo akamwambia: "Kwa sababu hukuisikiliza sauti ya Yehova, tazama, unaondoka kwangu, na hakika simba atakupiga na kukuua." Kisha akaondoka kando yake, na simba[h] akamkuta, akampiga na kumuua.[i]

37 Naye akamkuta mtu mwingine tena na kusema: "Tafadhali, nipige." Basi yule mtu akampiga, akampiga na kumtia majeraha.

38 Ndipo yule nabii akaenda, akasimama tuli akimngojea mfalme kando ya barabara, naye akakaa akiwa amejibadilisha sura[a] kwa kujifunga kitambaa juu ya macho yake. **39** Na ikawa kwamba mfalme alipokuwa anapita, akamwita mfalme na kusema:[b] "Mtumishi wako alienda mahali palipo na pigano kali sana; na tazama! mtu fulani alikuwa akitoka katika uwanja wa mapigano, kisha akaniletea mtu na kusema, 'Mlinde mtu huyu. Akitoweka kwa vyovyote, nafsi[c] yako itachukua mahali pa nafsi[d] yake, kama sivyo utapima talanta moja ya fedha.'[e] **40** Na ikawa kwamba mtumishi wako alipokuwa akitenda mambo hapa na pale, tazama, yule mtu alitoweka." Kwa hiyo mfalme wa Israeli akamwambia: "Hivyo ndivyo ilivyo hukumu yako mwenyewe. Wewe mwenyewe umeamua."[f] **41** Ndipo akavua haraka kile kitambaa kutoka juu ya macho yake, na mfalme wa Israeli akamtambua, kwamba alikuwa ni mmoja wa manabii.[g] **42** Sasa akamwambia: "Yehova amesema hivi, 'Kwa sababu umemwachilia kutoka mkononi mwako mtu niliyetengewa kwa ajili ya maangamizi,[h] lazima nafsi[i] yako ichukue mahali pa nafsi yake, na watu wako mahali pa watu wake.'"[j] **43** Hivyo mfalme wa Israeli akaenda zake nyumbani kwake, akiwa mwenye kinyongo na mwenye huzuni,[k] akafika Samaria.[l]

21 Na ikawa kwamba baada ya mambo hayo palikuwa na shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli, lililokuwa

SURA 20

a Yon 3:9

b Met 25:13

c 2Fa 10:15

d 1Fa 15:20
2Nya 16:4

e Kut 23:32

f 2Fa 2:3
Amo 7:14

g 1Fa 17:14

h 1Fa 13:24

i Met 16:25

Safu ya 2

a 2Sa 14:2

b 2Sa 12:1
2Sa 14:4

c Mwa 2:7
Law 17:11

d 2Fa 10:24
Mdo 12:19
Mdo 16:27

e Kut 21:30
Met 13:8

f Ayu 34:4
Lu 19:22
Ga 6:7

g 1Fa 20:35

h Law 27:29
Yos 6:18
1Sa 15:9
1Nya 2:7
Yer 48:10

i 1Fa 22:31
1Fa 22:35
2Nya 18:33

j 2Fa 6:24
2Fa 8:12
2Nya 18:16

k 1Fa 21:4
Zb 2:10

l 1Fa 16:29

kule Yezreeli,[a] kando ya ju-
mba la mfalme Ahabu, mfa-
lme wa Samaria. **2** Kwa hiyo
Ahabu akamwambia Nabothi:
"Nipe[b] shamba lako la mizabi-
bu,[c] ili liwe bustani[d] yangu ya
mboga,[e] kwa maana liko kari-
bu na nyumba yangu; nami ni-
takupa mahali pake shamba la
mizabibu lililo bora kuliko hilo.
Au ikiwa vema machoni pako,[f]
nitakupa pesa kama bei yake."
3 Lakini Nabothi akamwambia
Ahabu: "Ni jambo lisilowaziwa[g]
kwangu, kwa maoni ya Yeho-
va,[h] kwamba mimi nikupe fu-
ngu la urithi la mababu zangu."[i]
4 Hivyo Ahabu akaenda nyu-
mbani kwake, akiwa mwenye
kinyongo na mwenye huzuni
kwa sababu ya lile neno amba-
lo Nabothi Myezreeli alikuwa
amemwambia, aliposema: "Si-
takupa fungu la urithi la maba-
bu zangu." Kisha akalala kita-
ndani pake, akakaa akiwa ame-
geuza uso wake,[j] naye hakula
mkate.

5 Mwishowe Yezebeli[k] mke
wake akaingia kwake na kuse-
ma naye: "Kwa nini roho yako
imehuzunika,[l] nawe huli mka-
te?" **6** Naye akamwambia:
"Ni kwa sababu nilisema na Na-
bothi Myezreeli, nikamwambia,
'Nipe shamba lako la mizabi-
bu, nikupe pesa. Au, ukipenda,
acha nikupe shamba lingine la
mizabibu mahali pake.' Laki-
ni akasema, 'Sitakupa shamba
langu la mizabibu.'"[m] **7** Ndi-
po Yezebeli mke wake akamwa-
mbia: "Je, ni wewe unayetawa-
la ukiwa mfalme juu ya Israeli?[n]
Amka, ule mkate na moyo wako
ufurahi. Mimi mwenyewe ni-
takupa shamba la mizabibu la
Nabothi Myezreeli."[o] **8** Basi
mwanamke huyo akaandika ba-
rua[p] kwa jina la Ahabu, aka-
zitia muhuri[a] kwa muhuri wa
mfalme, akatuma barua hizo
kwa wanaume wazee[b] na watu
wenye vyeo waliokuwa katika
jiji lake, wakikaa na Nabothi.
9 Lakini akaandika katika ba-
rua hizo, akisema:[c] "Tangaze-
ni watu wafunge, mkamketi-
she Nabothi mbele ya watu.
10 Nanyi mwaketishe watu wa-
wili,[d] watu wasiofaa kitu,[e] mbe-
le yake, nao watoe ushahidi
juu yake,[f] wakisema, 'Umemla-
ani Mungu na mfalme!'[g] Na-
nyi mtoeni nje na kumpiga kwa
mawe ili afe."[h]

11 Basi watu wa jiji lake, wa-
naume wazee na watu wenye
vyeo waliokuwa wakikaa kati-
ka jiji lake, wakafanya kama
vile Yezebeli alivyokuwa ame-
tuma ujumbe kwao, kama ili-
vyoandikwa katika zile barua
alizowatumia.[i] **12** Wakata-
ngaza watu wafunge[j] na ku-
mketisha Nabothi mbele ya
watu. **13** Ndipo watu wawi-
li, watu wasiofaa kitu, wakai-
ngia, wakaketi mbele yake; ki-
sha wale watu wasiofaa kitu
wakaanza kutoa ushahidi juu
yake, yaani, Nabothi, mbele ya
watu, wakisema: "Nabothi ame-
mlaani Mungu na mfalme!"[k]
Kisha wakamtoa nje hadi mipa-
kani mwa jiji, wakampiga kwa
mawe, akafa.[l] **14** Sasa wakatu-
ma ujumbe kwa Yezebeli, waki-
sema: "Nabothi amepigwa kwa
mawe, akafa."[m]

15 Na ikawa kwamba mara
tu Yezebeli aliposikia kwamba
Nabothi amepigwa kwa mawe
akafa, mara moja Yezebeli aka-
mwambia Ahabu: "Ondoka, mi-
liki shamba la mizabibu la Na-
bothi, Myezreeli,[n] ambalo alika-
taa kukupa kwa pesa; kwa ma-
ana Nabothi hayuko hai tena,
bali amekufa." **16** Na ikawa

SURA 21
a Yos 19:18
1Fa 18:45
Ho 2:22
b Kut 20:17
Kum 5:21
Hab 2:9
Lu 12:15
Ro 7:7
Yak 1:14
2Pe 2:14
c 1Sa 8:14
d Mhu 2:5
e Kum 11:10
f Mwa 16:6
g Law 25:18
Zb 97:10
Amo 5:15
h Yos 22:5
1Sa 24:6
1Sa 26:11
i Law 25:23
Hes 36:7
Eze 46:18
j Met 15:13
Met 18:14
k 1Fa 16:31
1Fa 18:4
1Fa 19:2
1Fa 21:25
2Fa 9:34
l Ne 2:2
m 1Fa 21:3
n 1Sa 8:14
o Mik 2:1
Mik 7:3
p 2Sa 11:14

Safu ya 2
a Ne 9:38
Est 8:8
b Hes 11:16
Kum 16:18
c Met 6:18
d Kum 17:6
e 1Sa 2:12
2Sa 20:1
Met 17:23
f Kut 20:16
Kum 5:20
Met 6:19
Met 24:28
Isa 32:7
Mdo 6:13
g Kut 22:28
Law 24:16
Mt 26:65
Mdo 23:5
h Law 24:16
Yoh 10:33
Mdo 7:58
i Kut 23:1
Law 19:15
j Isa 58:4
k 1Fa 21:10
Mhu 3:16
Amo 5:12
Hab 1:4
l 2Fa 9:26
Mhu 4:1
m Mhu 5:8
Mhu 8:14
Hab 1:13
n 1Fa 21:7
Met 4:17
Yer 22:17

kwamba mara tu Ahabu alipositkia kwamba Nabothi amekufa, Ahabu akaondoka mara moja ili ashuke kwenda katika lile shamba la mizabibu la Nabothi, Myezreeli, alimiliki.[a]

17 Na neno la Yehova[b] likamjia Eliya[c] Mtishbi, likisema: **18** "Ondoka, nenda ukutane na Ahabu mfalme wa Israeli, aliye katika Samaria.[d] Tazama, yupo katika shamba la mizabibu la Nabothi, mahali ambapo ameenda kulimiliki. **19** Nawe unapaswa kumwambia, ukisema, 'Yehova amesema hivi: "Je, umeua[e] na pia ukamiliki?"'[f] Nawe unapaswa kumwambia, ukisema, 'Yehova amesema hivi: "Mahali[g] ambapo mbwa waliiramba damu ya Nabothi, mbwa watairamba damu yako, ndiyo, damu yako."'"[h]

20 Na Ahabu akamwambia Eliya: "Je, umenipata, ewe adui yangu?"[i] naye akasema: "Nimekupata. 'Kwa sababu umejiuza ili kufanya yaliyo mabaya machoni pa Yehova,[j] **21** tazama, ninaleta msiba juu yako;[k] nami nitafagia kabisa nikikufuata nyuma yako[l] na kukatilia mbali kutoka kwa Ahabu yeyote anayekojoa ukutani[m] na asiye na uwezo na asiye na thamani katika Israeli. **22** Nami nitaifanya nyumba yako kuwa kama nyumba ya Yeroboamu[n] mwana wa Nebati na kama nyumba ya Baasha[o] mwana wa Ahiya, kwa ajili ya kosa ambalo umekosea, kisha kusababisha Israeli kutenda dhambi.'[p] **23** Na pia Yehova amesema hivi kuhusu Yezebeli, 'Mbwa watamla Yezebeli katika uwanja wa shamba la Yezreeli.[q] **24** Mtu yeyote wa Ahabu anayekufa jijini mbwa watamla; na yeyote anayekufa shambani ndege wa mbinguni watamla.[a] **25** Hakuna kamwe mtu yeyote ambaye amepata kuwa kama Ahabu,[b] aliyejiuza ili kufanya yaliyo mabaya machoni pa Yehova, ambaye Yezebeli[c] mke wake alimchochea.[d] **26** Naye akatenda kwa njia yenye kuchukiza sana kwa kufuata sanamu za mavi,[e] kama yale yote ambayo Waamori walikuwa wametenda, ambao Yehova aliwafukuza kutoka mbele ya wana wa Israeli.'"[f]

27 Na ikawa kwamba mara tu Ahabu alipoyasikia maneno hayo, akayararua mavazi yake, akavaa nguo za magunia[g] mwilini mwake; naye akaanza kufunga, akaendelea kulala katika nguo za magunia, akatembea kwa huzuni.[h] **28** Na neno la Yehova likamjia Eliya, Mtishbi, likisema: **29** "Je, umeona jinsi ambavyo Ahabu amejinyenyekeza kwa ajili yangu?[i] Kwa sababu amejinyenyekeza kwa ajili yangu, sitauleta ule msiba katika siku zake.[j] Katika siku za mwana wake nitauleta msiba ule juu ya nyumba yake."[k]

22 Na kwa miaka mitatu wakaendelea kuishi bila vita kati ya Siria na Israeli. **2** Na ikawa kwamba katika mwaka wa tatu, Yehoshafati[l] mfalme wa Yuda akashuka, akaenda kwa mfalme wa Israeli. **3** Ndipo mfalme wa Israeli akawaambia watumishi wake: "Je, kweli hamjui kwamba Ramothi-gileadi[m] ni jiji letu? Na bado tunasitasita kulichukua kutoka mkononi mwa mfalme wa Siria." **4** Naye akamwambia Yehoshafati: "Je, utaenda pamoja nami kupigana kule Ramothi-gileadi?"[n] Ndipo Yehoshafati akamwambia mfalme

SURA 21
a Zb 50:18 Hab 2:12 Ro 1:32 2Pe 2:15
b Zb 9:12 Isa 26:21
c 1Fa 17:1
d 1Fa 16:29
e Mwa 4:10
f Hab 2:9
g Kut 21:23 Zb 7:15
h 1Fa 22:38 2Fa 9:25 Mt 7:2
i 1Fa 18:17 Amo 5:10 Ga 4:16
j 1Fa 16:30
k 2Fa 9:7
l Kut 20:5 2Fa 9:8 2Fa 10:7
m 2Fa 10:17 2Fa 10:30
n 1Fa 15:29
o 1Fa 16:3 1Fa 16:11
p 1Fa 16:26
q 2Fa 9:10 2Fa 9:35 Zb 7:16

Safu ya 2
a 1Fa 14:11 1Fa 16:4 Yer 15:3 Ufu 19:18
b 1Fa 16:30
c 1Fa 16:31
d Kum 13:6 Amu 16:16 2Nya 22:3 Ufu 2:20
e 1Sa 12:21 Zb 96:5 Yer 10:14 1Ko 8:4
f Kut 23:28 Kum 9:5 2Nya 33:2
g 1Fa 20:31 2Ko 7:10
h Met 15:13
i Zb 78:34
j Zb 86:15 Mik 7:18
k Kut 20:5 2Fa 9:25 2Fa 10:7 2Fa 10:11

SURA 22
l 1Fa 15:24 2Nya 18:3
m Kum 4:43 Yos 20:8 1Fa 4:13
n 2Nya 18:2

wa Israeli: "Mimi ni sawa na
wewe. Watu wangu ni sawa na
watu wako.[a] Farasi zangu ni
sawa na farasi zako."
5 Hata hivyo, Yehoshafati
akaendelea kumwambia mfa-
lme wa Israeli: "Tafadhali, kwa-
nza kabisa uliza[b] neno la Yeho-
va." **6** Kwa hiyo mfalme wa
Israeli akawakusanya manabii
pamoja,[c] karibu watu mia nne,
akawaambia: "Je, niende kupi-
ga vita juu ya Ramothi-gileadi,
au nijiepushe?" Nao wakaanza
kusema: "Panda uende,[d] na Ye-
hova atalitia jiji hilo mkononi
mwa mfalme."
7 Lakini Yehoshafati akase-
ma: "Je, hayupo hapa tena nabii
wa Yehova? Basi na tuulize ku-
pitia yeye."[e] **8** Ndipo mfalme
wa Israeli akamwambia Yeho-
shafati: "Bado kuna mtu mmo-
ja ambaye tunaweza kumuuliz-
za Yehova kupitia yeye;[f] laki-
ni hakika mimi ninamchukia,[g]
kwa maana yeye hatoi unabii
wa mambo mema kunihusu
mimi, ila mabaya[h]—Mikaya
mwana wa Imla." Hata hivyo,
Yehoshafati akasema: "Mfalme
asiseme jambo kama hilo."[i]
9 Basi mfalme wa Israeli
akamwita ofisa[j] fulani wa ma-
kao ya mfalme na kusema:
"Mlete haraka Mikaya mwa-
na wa Imla."[k] **10** Sasa mfalme
wa Israeli na Yehoshafati mfa-
lme wa Yuda walikuwa wame-
keti kila mmoja juu ya kiti cha-
ke cha ufalme, wakiwa wame-
vaa mavazi ya kifalme,[l] kati-
ka uwanja wa kupuria kwenye
mwingilio wa lango la Samaria;
na manabii wote walikuwa wa-
kitenda kama manabii mbele
yao.[m] **11** Ndipo Sedekia mwa-
na wa Kenaana akajitengene-
zea pembe za chuma na kuse-
ma: "Yehova amesema hivi,[n]
'Kwa kutumia hizi utawasuku-
ma Wasiria mpaka uwaanga-
mize.'"[a] **12** Na wale manabii
wengine wote walikuwa waki-
toa unabii kama huo, wakise-
ma: "Panda uende Ramothi-gi-
leadi, upate mafanikio; na Yeho-
va hakika atalitia jiji lile mko-
noni mwa mfalme."[b]
13 Na yule mjumbe aliyee-
nda kumwita Mikaya akamwa-
mbia, akisema: "Tazama, sasa!
Maneno ya manabii kwa ka-
uli moja ni mema kwa mfa-
lme. Tafadhali, neno lako na
liwe kama neno la mmoja wao,
nawe useme mema."[c] **14** La-
kini Mikaya akasema: "Kama
Yehova anavyoishi,[d] lile amba-
lo Yehova ataniambia, hilo ndi-
lo nitakalosema."[e] **15** Ndipo
akaingia kwa mfalme, naye
mfalme akamwambia: "Mika-
ya, je, twende kupiga vita juu
ya Ramothi-gileadi, au tuji-
epushe?" Mara moja akamwa-
mbia: "Panda uende na kufani-
kiwa; na Yehova atalitia mko-
noni mwa mfalme."[f] **16** Kwa
hiyo mfalme akamwambia: "Ni-
nakuapisha mara ngapi kwa-
mba usiniambie jambo lolote ila
kweli katika jina la Yehova?"[g]
17 Basi akasema: "Hakika ni-
nawaona Israeli wote wameta-
wanyika[h] juu ya milima, kama
kondoo wasio na mchungaji.[i]
Na Yehova akasema: 'Hawa ha-
wana mabwana. Kila mmoja
na arudi kwa amani nyumbani
kwake.'"[j]
18 Ndipo mfalme wa Israeli
9 Mwishowe wakaanza kuambiana: "Jambo tunalofanya si sawa. Leo ni siku ya habari njema![k] Tukisitasita, na tungojee mpaka nuru ya asubuhi, hatia itatupata pia.[l] Basi sasa njooni, tuingie, tupeleke habari nyumbani kwa mfalme." **10** Basi wakaenda, wakawaita watunza-malango[m] wa jiji na kuwaletea habari, wakisema: "Tulingia katika kambi ya Wasiria, na, tazama! hapakuwa na mtu yeyote humo wala sauti ya mwanadamu, lakini farasi peke yao waliofungwa na punda waliofungwa na mahema kama walivyoyaacha."[a] **11** Mara moja wale watunza-malango wakaita na kupeleka habari ndani nyumbani kwa mfalme.

12 Mfalme akasimama mara moja wakati wa usiku, akawaambia watumishi[b] wake: "Tafadhali, acheni niwaambie yale ambayo Wasiria wametufanyia.[c] Wanajua vema kwamba tuna njaa;[d] na basi walitoka kambini ili wajifiche shambani,[e] wakisema, 'Watatoka jijini, nasi tutawakamata wakiwa hai, nasi tutaingia jijini.'" **13** Ndipo mmoja wa watumishi wake akajibu na kusema: "Tafadhali, acha wachukue farasi watano kati ya wale waliobaki ambao wamebaki jijini.[f] Tazama! Wao ni sawa na umati wote wa Israeli ambao umebaki ndani yake. Tazama! Wao ni kama umati wote wa Israeli ambao umeangamia.[g] Nasi tutume watu tuone." **14** Kwa hiyo wakachukua magari mawili pamoja na farasi na mfalme akawatuma kuifuata kambi ya Wasiria, akisema: "Nendeni mwone." **15** Ndipo wakawafuata mpaka Yordani; na tazama! njia yote ilijaa mavazi na vyombo[h] ambavyo Wasiria walikuwa wamevitupa walipokuwa wanakimbia.[i] Kisha wale wajumbe wakarudi na kumletea mfalme habari.

16 Na watu wakaenda na kuipora[j] kambi ya Wasiria; basi kipimo kimoja cha sea cha unga laini kikawa na thamani ya shekeli moja, na vipimo viwili vya

SURA 7

a 2Fa 6:25
b Omb 4:9
c Met 20:12
d Kum 28:7
2Sa 5:24
2Fa 19:7
e 1Fa 10:29
2Nya 1:17
f 2Nya 12:2
g Zb 48:5
Met 28:1
h Zb 33:17
Met 21:31
i Mwa 2:7
j Yer 41:8
k Nah 1:15
1Ko 10:24
Flp 2:4
1Th 5:15
l 1Ti 6:10
m 2Sa 18:26
Zb 127:1
Mk 13:34

Safu ya 2

a 2Fa 7:7
b 2Fa 6:8
c Met 14:15
d 2Fa 6:25
2Fa 6:29
e Yos 8:4
Yos 8:12
Amu 20:29
Amu 20:37
f 2Fa 6:25
g Omb 4:9
h Est 1:7
Isa 22:24
i Zb 68:12
Isa 2:20
Mt 16:26
j 2Nya 20:25
Zb 68:12
Isa 33:1

sea vya shayiri vikawa na thamani ya shekeli moja, kulingana na lile neno[a] la Yehova. **17** Na mfalme alikuwa amemweka yule amiri msaidizi ambaye alikuwa amejiegemeza[b] juu ya mkono wake asimamie njia ya lango; na watu wakaendelea kumkanyaga[c] katika njia ya lango, hata akafa, kama alivyokuwa amesema yule mtu wa Mungu wa kweli,[d] aliposema wakati mfalme aliposhuka kumjia. **18** Basi ikawa kama alivyosema yule mtu wa Mungu wa kweli kwa mfalme, akisema: "Vipimo viwili vya sea vya shayiri vyenye thamani ya shekeli moja na kipimo kimoja cha sea cha unga laini chenye thamani ya shekeli moja ndivyo itakavyokuwa kesho wakati kama huu katika njia ya lango la Samaria."[e] **19** Lakini yule amiri msaidizi akamjibu mtu wa Mungu wa kweli na kusema: "Hata ikiwa Yehova angefanya madirisha mbinguni, je, ingeweza kutokea kulingana na neno hili?"[f] Naye akasema: "Tazama, wewe unaliona hilo kwa macho yako, lakini wewe hutakula kutokana nalo."[g] **20** Basi ikawa hivyo kwake,[h] wakati watu walipoendelea kumkanyaga[i] katika njia ya lango, hata akafa.

8 Na Elisha alikuwa amemwambia yule mwanamke ambaye alikuwa amemfufua mwana wake,[j] na kusema: "Ondoka uende, wewe pamoja na nyumba yako, ukae ugenini popote unapoweza kukaa ugenini;[k] kwa kuwa Yehova ametangaza kuwe na njaa,[l] na zaidi ya hayo, itakuja juu ya nchi kwa miaka saba."[m] **2** Basi yule mwanamke akaondoka, akafanya kulingana na neno la yule mtu wa Mungu wa kweli, akaenda,[n] yeye pamoja na nyumba yake,[a] akaanza kukaa ugenini katika nchi ya Wafilisti[b] kwa miaka saba.

3 Na ikawa kwamba mwishoni mwa miaka saba yule mwanamke akarudi kutoka katika nchi ya Wafilisti, akaenda kumlilia mfalme[c] kwa ajili ya nyumba yake na kwa ajili ya shamba lake. **4** Sasa mfalme alikuwa akisema na Gehazi[d] mtumishi wa yule mtu wa Mungu wa kweli, kusema: "Tafadhali, nisimulie mambo yote makuu ambayo Elisha amefanya."[e] **5** Na ikawa kwamba alipokuwa akimsimulia mfalme jinsi alivyokuwa amemfufua mtu aliyekufa,[f] tazama, yule mwanamke aliyekuwa amemfufulia mwana wake alikuwa akimlilia mfalme kwa ajili ya nyumba yake na kwa ajili ya shamba[g] lake. Mara moja Gehazi akasema: "Bwana[h] wangu mfalme, huyu ndiye yule mwanamke, na huyu ndiye mwana wake ambaye Elisha alimfufua." **6** Ndipo mfalme akamuuliza yule mwanamke, naye akamsimulia hadithi ile.[i] Kisha mfalme akampa mwanamke huyo ofisa wa makao ya mfalme,[j] akisema: "Rudisha mali yote ya mwanamke huyu na mazao yote ya shamba lake tangu siku alipotoka katika nchi mpaka sasa."[k]

7 Na Elisha akaenda Damasko;[l] na Ben-hadadi[m] mfalme wa Siria alikuwa mgonjwa. Basi akaletewa habari, ikisema: "Yule mtu wa Mungu[n] wa kweli amefika hapa." **8** Kwa hiyo mfalme akamwambia Hazaeli:[o] "Chukua zawadi[p] mkononi mwako, nenda umpokee yule mtu wa Mungu wa kweli, nawe uulize[q] Yehova kupitia kwake,

SURA 7

a Hes 23:19
2Fa 7:1
Isa 44:26
Isa 55:11
b 2Fa 5:18
c 2Fa 9:33
Isa 25:10
d Kum 32:35
2Fa 7:2
2Nya 36:16
Isa 5:24
Isa 28:22
Nah 1:2
e 2Fa 7:1
Isa 44:26
f Hes 20:12
Zb 78:19
g 2Fa 7:2
h 2Nya 20:20
i Isa 41:25

SURA 8

j 2Fa 4:35
k Mwa 12:10
Mwa 26:1
Mwa 47:4
Ru 1:1
l Law 26:19
Kum 28:23
2Sa 21:1
1Fa 17:1
Zb 105:16
Mdo 11:28
m Mwa 41:27
2Sa 24:13
Amo 3:2
n Met 27:12

Safu ya 2

a Mwa 15:3
1Ti 5:8
b Yos 13:3
1Sa 27:1
c 1Sa 8:5
2Sa 14:4
2Fa 6:26
Lu 18:3
d 2Fa 4:12
e 2Fa 2:14
2Fa 2:20
2Fa 3:17
2Fa 4:4
2Fa 5:14
2Fa 5:27
2Fa 6:6
2Fa 7:1
f 2Fa 4:35
g Hes 36:9
h 1Sa 26:17
2Fa 6:26
1Pe 2:17
i 2Fa 4:32
j 2Fa 9:32
k Zb 82:3
Met 21:1
Met 29:4
Met 31:9
l Isa 7:8
m 1Fa 20:1
2Fa 6:24
n 1Fa 17:24
o 1Fa 19:15
p 1Sa 9:8
1Fa 14:3
2Fa 5:5
q Mwa 25:22
1Fa 14:2
2Fa 3:11
2Fa 22:13

na kusema, ‘Je, nitapona ugonjwa huu?’” **9** Basi Hazaeli akaenda kumpokea, akachukua zawadi mkononi mwake, naam, kila namna ya kitu chema cha Damasko, mzigo wa ngamia 40, akaja na kusimama mbele yake, akasema: “Mwana[a] wako, Ben-hadadi, mfalme wa Siria, amenituma kwako, kusema, ‘Je, nitapona ugonjwa huu?’” **10** Ndipo Elisha akamwambia: “Nenda, mwambie, ‘Utapona hakika,’ na Yehova amenionyesha[b] kwamba atakufa hakika.”[c] **11** Naye akamkazia macho, akayakaza mpaka akaona haya. Kisha yule mtu wa Mungu wa kweli akaanza kulia.[d] **12** Kwa hiyo Hazaeli akasema: “Kwa nini bwana wangu analia?” Naye akasema: “Kwa sababu ninajua vema mabaya[e] utakayowatendea wana wa Israeli. Utateketeza kwa moto mahali pao penye ngome, na wanaume wao walio bora utawaua kwa upanga, na watoto wao utawavunja vipande-vipande,[f] na wanawake wao wenye mimba utawapasua.”[g] **13** Basi Hazaeli akasema: “Mtumishi wako ni nani, ambaye ni mbwa[h] tu, ndipo aweze kufanya jambo hili kuu?” Lakini Elisha akasema: “Yehova amenionyesha wewe kuwa mfalme juu ya Siria.”[i]

14 Kisha akatoka kwa Elisha, akaenda kwa bwana wake, ambaye sasa alimuuliza: “Elisha alikuambia nini?” Naye akasema: “Aliniambia, ‘Hakika utapona.’”[j] **15** Na ikawa kwamba kesho yake akachukua tandiko lenye mapambo, akalichovya ndani ya maji, akalifunika juu ya uso wake,[k] hata akafa.[l] Na Hazaeli[m] akaanza kutawala mahali pake.

SURA 8

a 1Sa 25:8
2Fa 6:21
2Fa 13:14
b Isa 44:26
Amo 3:7
c 2Fa 8:15
d Yer 9:1
Lu 19:41
Mdo 20:19
e 2Fa 10:32
2Fa 12:17
2Fa 13:3
Amo 1:3
f Kum 28:45
Kum 28:63
2Fa 15:16
Ho 10:14
g Isa 13:16
Ho 13:16
Amo 1:13
h 1Sa 17:43
2Sa 9:8
Zb 22:20
i 1Sa 2:7
1Fa 19:15
j 2Fa 8:10
k Zb 36:1
Mik 2:1
l 1Fa 16:10
2Fa 11:1
2Fa 15:10
Isa 33:1
m 1Fa 19:15

Safu ya 2

a 2Fa 1:17
b 1Fa 22:50
2Nya 21:3
c 2Nya 21:5
d 1Fa 12:28
1Fa 16:32
e 1Fa 16:33
1Fa 21:25
2Fa 21:3
2Nya 21:13
f 2Fa 8:26
2Nya 18:1
2Nya 21:6
g Mwa 49:10
h 2Sa 7:16
2Nya 21:7
i 1Fa 11:36
Zb 132:17
Lu 1:69
Mdo 15:16
j Mwa 27:40
2Sa 8:14
2Fa 3:9
2Nya 21:8
k 2Sa 8:14
1Fa 22:47
l Yos 21:13
2Fa 19:8
2Nya 21:10
m 1Fa 14:29
1Fa 15:23
2Fa 15:6
2Fa 15:36
n 1Fa 2:10
1Fa 11:43
1Fa 14:31
2Nya 21:19
o 2Nya 21:20
p 1Nya 3:11
2Nya 21:17

16 Na katika mwaka wa tano wa Yehoramu[a] mwana wa Ahabu mfalme wa Israeli, Yehoshafati alipokuwa mfalme wa Yuda, Yehoramu[b] mwana wa Yehoshafati mfalme wa Yuda akawa mfalme. **17** Alikuwa na umri wa miaka 32 alipoanza kuwa mfalme, naye akatawala miaka 8 katika Yerusalemu.[c] **18** Naye akaendelea kutembea katika njia ya wafalme wa Israeli,[d] kama walivyofanya wale wa nyumba ya Ahabu;[e] kwa maana binti ya Ahabu ndiye aliyekuwa mke wake,[f] naye akaendelea kufanya yaliyokuwa mabaya machoni pa Yehova. **19** Na Yehova hakutaka kuharibu Yuda[g] kwa sababu ya Daudi mtumishi wake,[h] kama alivyokuwa ameahidi kumpa taa,[i] yeye na wanawe sikuzote.

20 Katika siku zake Edomu[j] waliasi kutoka chini ya mkono wa Yuda, nao wakaweka mfalme[k] atawale juu yao. **21** Basi Yehoramu akavuka mpaka Sairi, pia magari yote pamoja naye. Na ikawa kwamba yeye akaondoka wakati wa usiku, akawapiga na kuwaua Waedomu waliokuwa wamemzunguka na wale wakuu wa magari; na watu wakakimbia kwenda katika mahema yao. **22** Lakini Edomu wakaendelea kuasi kutoka chini ya mkono wa Yuda mpaka leo hii. Wakati huo ndipo Libna[l] wakaanza kuasi.

23 Na mambo mengine ya Yehoramu na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa katika kitabu[m] cha mambo ya siku za wafalme wa Yuda? **24** Mwishowe Yehoramu akalala pamoja na mababu zake,[n] akazikwa pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi.[o] Na Ahazia[p] mwana

wake akaanza kutawala mahali pake.

25 Katika mwaka wa kumi na mbili wa Yehoramu mwana wa Ahabu mfalme wa Israeli, Ahazia mwana wa Yehoramu mfalme wa Yuda akawa mfalme.[a] **26** Ahazia alikuwa na umri wa miaka 22 alipoanza kutawala, naye akatawala mwaka mmoja katika Yerusalemu.[b] Na jina la mama yake lilikuwa Athalia[c] mjukuu wa Omri[d] mfalme wa Israeli. **27** Naye akaendelea kutembea katika njia ya nyumba ya Ahabu,[e] akazidi kufanya yaliyokuwa mabaya machoni pa Yehova,[f] kama nyumba ya Ahabu, kwa maana alikuwa mtu wa jamaa ya nyumba ya Ahabu kupitia ndoa.[g] **28** Basi akaenda pamoja na Yehoramu mwana wa Ahabu kupigana vita na Hazaeli[h] mfalme wa Siria kule Ramothi-gileadi,[i] lakini Wasiria wakampiga[j] Yehoramu. **29** Kwa hiyo Yehoramu[k] mfalme akarudi Yezreeli[l] ili apone yale majeraha waliyomtia Wasiria kule Rama alipopigana na Hazaeli mfalme wa Siria. Naye Ahazia[m] mwana wa Yehoramu mfalme wa Yuda akashuka ili amwone Yehoramu mwana wa Ahabu katika Yezreeli, kwa maana alikuwa mgonjwa.

9 Na Elisha nabii akamwita mmoja wa wana[n] wa manabii, kisha akamwambia: "Jifunge viuno[o] vyako uchukue chupa[p] hii ya mafuta mkononi mwako, uende Ramothi-gileadi.[q] **2** Utakapoingia humo, mwone Yehu[r] mwana wa Yehoshafati mwana wa Nimshi humo; nawe uingie ndani na kumsimamisha kutoka katikati ya ndugu zake, umwingize katika chumba cha ndani kabisa.[s] **3** Nawe uchukue chupa ya mafuta uyamimine juu ya kichwa[a] chake na kusema, 'Yehova amesema hivi: "Ninakutia mafuta[b] uwe mfalme[c] juu ya Israeli."' Nawe ufungue mlango, ukimbie, wala usingoje."

4 Na yule mtumishi, mtumishi wa nabii, akaondoka kwenda Ramothi-gileadi. **5** Alipoingia, tazama, wakuu wa majeshi walikuwa wameketi. Akasema: "Nina neno kwa ajili yako,[d] ewe mkuu." Ndipo Yehu akasema: "Ni kwa ajili ya nani kati yetu sote?" Kisha akasema: "Kwa ajili yako, ewe mkuu." **6** Basi akasimama, akaingia ndani ya nyumba; naye akamimina yale mafuta juu ya kichwa chake na kumwambia: "Yehova Mungu wa Israeli amesema hivi, 'Ninakutia mafuta uwe mfalme[e] juu ya watu wa Yehova,[f] yaani, juu ya Israeli. **7** Nawe uipige nyumba ya Ahabu bwana wako, nami lazima nilipize kisasi[g] damu ya watumishi wangu manabii na damu ya watumishi wote wa Yehova mkononi mwa Yezebeli.[h] **8** Na nyumba yote ya Ahabu lazima iangamie; nami nitakatilia mbali kutoka kwa Ahabu[i] mtu yeyote anayekojoa ukutani[j] na yeyote asiye na uwezo na asiye na thamani[k] katika Israeli. **9** Nami nitaifanya nyumba ya Ahabu kuwa kama nyumba ya Yeroboamu[l] mwana wa Nebati na kama nyumba ya Baasha[m] mwana wa Ahiya. **10** Na mbwa watamla[n] Yezebeli katika sehemu ya shamba kule Yezreeli, wala hakuna atakayemzika.'" Kisha akafungua mlango, akakimbia.[o]

11 Ndipo Yehu akatoka nje, akawaendea watumishi wa bwana wake, nao wakaanza ku-

SURA 8

a 2Fa 9:29
2Nya 22:1
b 2Nya 22:2
c 2Fa 8:18
2Fa 11:1
2Fa 11:13
2Fa 11:16
d 1Fa 16:16
1Fa 16:23
1Fa 16:27
2Nya 22:2
e 1Fa 16:33
2Nya 22:3
f 2Fa 19:22
g 2Fa 8:18
2Ko 6:14
h 2Fa 9:15
2Nya 22:5
i Yos 21:38
1Fa 22:3
j 1Fa 19:17
k 2Fa 9:15
l Yos 19:18
1Fa 21:1
2Nya 22:6
m 2Fa 9:16

SURA 9

n 2Fa 4:1
2Fa 6:1
o 1Fa 18:46
2Fa 4:29
Lu 12:35
p 1Sa 10:1
q 2Fa 8:28
2Nya 22:5
r 1Fa 19:17
s 1Fa 20:30
1Fa 22:25

Safu ya 2

a Kut 29:7
1Fa 19:16
b 2Nya 22:7
c Yer 27:5
Da 2:21
d Amu 3:19
e 1Fa 19:16
2Nya 22:7
f 1Fa 16:2
g Kum 32:35
Kum 32:43
Zb 94:1
Lu 18:7
Ro 12:19
Ro 13:4
Ebr 10:30
h 1Fa 18:4
1Fa 19:2
1Fa 21:15
1Fa 21:25
i 1Fa 21:21
j 1Fa 14:10
k Kum 32:36
1Fa 21:21
l 1Fa 15:29
m 1Fa 16:11
n 1Fa 21:23
o 2Fa 9:3

muuliza: “Je, ni salama?[a] Kwa
nini huyu mwenda-wazimu[b] ali-
kuja kwako?” Lakini akawaa-
mbia: “Ninyi mnajua vema mtu
huyo na namna yake ya kuo-
ngea.” **12** Lakini wakasema:
“Si kweli! Tafadhali tuambie.”
Ndipo akasema: “Aliniambia
hivi na vile, akisema, ‘Yehova
amesema hivi: “Ninakutia ma-
futa uwe mfalme juu ya Israe-
li.”’”[c] **13** Kwa hiyo wakafa-
nya haraka, kila mmoja wao
akachukua vazi[d] lake na kuli-
tandika chini yake juu ya zile
ngazi zilizo wazi, nao wakaa-
nza kupiga baragumu,[e] wakise-
ma: “Yehu amekuwa mfalme!”[f]
14 Na Yehu[g] mwana wa Yeho-
shafati mwana wa Nimshi[h] aka-
panga hila[i] juu ya Yehoramu.

Na Yehoramu alikuwa akili-
nda kule Ramothi-gileadi,[j] yeye
na Israeli wote, kwa sababu
ya Hazaeli[k] mfalme wa Siria.
15 Baadaye Yehoramu[l] mfalme
akarudi kule Yezreeli[m] ili apone
yale majeraha ambayo Wasiria
walimtia alipopigana na Hazae-
li mfalme wa Siria.[n]

Sasa Yehu akasema: “Nafsi
yenu ikikubali,[o] msiache ye-
yote akimbie kutoka jijini na
kupeleka habari Yezreeli.”
16 Na Yehu akaanza kupanda,
akaenda Yezreeli; kwa maa-
na Yehoramu alikuwa amela-
la huko, na Ahazia[p] mfalme
wa Yuda alikuwa ameshuka
kwenda kumwona Yehoramu.
17 Na mlinzi[q] alikuwa amesi-
mama juu ya mnara[r] katika Ye-
zreeli,[s] naye akaona umati una-
osukasuka wa watu wa Yehu
alipokuwa akija, naye akase-
ma mara moja: “Ninaona umati
unaosukasuka wa watu.” Ndipo
Yehoramu akasema: “Chukua
askari mpanda-farasi, umtu-
me awapokee, naye aseme, ‘Je,

SURA 9

a 2Fa 4:26
b 1Sa 21:14
c 2Fa 9:6
d Mt 21:7
e 2Sa 15:10
1Fa 1:34
f 1Fa 1:39
g 1Fa 19:16
h 2Fa 9:2
i 2Fa 10:9
j 1Fa 22:3
2Fa 8:28
k 1Fa 19:15
2Fa 8:15
2Fa 10:32
l 2Fa 8:29
m Yos 19:18
1Fa 21:1
n 2Nya 22:6
o Met 20:18
p 2Nya 22:7
q Isa 21:6
Isa 62:6
Eze 33:2
r 2Nya 14:7
s 1Fa 21:1

Safu ya 2

a 1Sa 16:4
1Fa 2:13
b Isa 48:22
Ro 3:17
c 2Sa 18:24
2Sa 18:26
d Isa 57:21
e 1Fa 19:16
f 2Fa 9:2
g Zek 12:4
h Mik 1:13
i 2Fa 8:25
2Fa 8:29
2Nya 22:7
j 1Fa 21:1
1Fa 21:15
1Fa 21:19
k Isa 48:22
Isa 57:21
Isa 59:8
Yer 16:5
Ro 3:17
l 1Fa 16:31
1Fa 18:4
1Fa 19:2
1Fa 21:7
Ufu 9:21
m Law 20:6
Kum 18:10
1Fa 18:19
Mal 3:5
n 2Fa 11:14
o Zb 7:12

kuna amani?’”[a] **18** Basi mpa-
nda-farasi akaenda kumpokea
na kusema: “Mfalme amesema
hivi, ‘Je, kuna amani?’” Laki-
ni Yehu akasema: “Una nini na
‘amani’?[b] Nenda nyuma yangu!”

Na yule mlinzi[c] akaendelea
kutoa habari, akisema: “Yule
mjumbe aliwafikia, lakini ha-
kurudi.” **19** Kwa hiyo aka-
tuma mpanda-farasi wa pili,
ambaye, alipowafikia, alisema:
“Mfalme amesema hivi, ‘Je,
kuna amani?’” Lakini Yehu
akasema: “Una nini na ‘aman-
ni’?[d] Nenda nyuma yangu!”

20 Na yule mlinzi akaende-
lea kutoa habari, akisema: “Ali-
wafikia, lakini hakurudi; na ue-
ndeshaji ule ni kama uendesha-
ji wa Yehu[e] mjukuu wa Nimshi,[f]
kwa maana yeye huendesha ki-
wazimu.”[g] **21** Ndipo Yehora-
mu akasema: “Fungeni!”[h] Basi
gari lake la vita likafungwa,
na Yehoramu mfalme wa Israe-
li na Ahazia[i] mfalme wa Yuda
wakatoka, kila mmoja wao aki-
wa ndani ya gari lake la vita.
Walipoendelea kwenda kumpo-
kea Yehu, wakamkuta katika
sehemu ya shamba la Nabothi,[j]
Myezreeli.

22 Na ikawa kwamba mara
tu Yehoramu alipomwona Yehu,
mara moja akasema: “Je, kuna
amani, Yehu?” Lakini yeye
akasema: “Kunaweza kuwa na
amani[k] gani wakati kungali na
uasherati wa Yezebeli[l] mama
yako na ulozi wake mwingi?”[m]
23 Mara moja Yehoramu aka-
geuka kwa mikono yake, ili
akimbie, na kumwambia Aha-
zia: “Kuna udanganyifu,[n] Aha-
zia!” **24** Na Yehu akatia upi-
nde[o] mkononi mwake, akampi-
ga Yehoramu katikati ya mi-
kono, hivi kwamba ule mshale
ukatokea moyoni mwake, naye

akaanguka ndani ya gari lake la
vita.[a] **25** Sasa akamwambia
Bidkari amiri msaidizi wake:[b]
"Mwinue; mtupe katika ile se-
hemu ya shamba la Nabothi,
Myezreeli;[c] kwa maana kumbu-
ka: Mimi na wewe tulikuwa tu-
kiendesha makundi ya magari
ya farasi nyuma ya Ahabu baba
yake, na Yehova akatangaza[d]
hivi juu yake: **26** '"Hakika ni-
liona jana damu[e] ya Nabothi na
damu ya wanawe,"[f] asema Ye-
hova, "nami hakika nitakulipa[g]
wewe katika sehemu hii ya sha-
mba," asema Yehova.' Basi sasa,
mwinue; mtupe katika ile se-
hemu ya shamba kulingana na
neno la Yehova."[h]

27 Na Ahazia[i] mfalme wa
Yuda akaona hilo, akaanza ku-
kimbia kupitia njia ya busta-
ni ya nyumba.[j] (Baadaye Yehu
akamfuatilia na kusema: "Yeye
pia! Mpigeni!" Kwa hiyo waka-
mpiga alipokuwa ndani ya gari
kwenye njia inayopanda kwe-
nda Guri, lililo kando ya Ible-
amu.[k] Naye akaendelea kuki-
mbia kwenda Megido,[l] akafa
huko.[m] **28** Ndipo watumishi
wake wakambeba ndani ya gari
mpaka Yerusalemu, na hivyo
wakamzika katika kaburi lake
pamoja na mababu zake kati-
ka Jiji la Daudi.[n] **29** Na ili-
kuwa katika mwaka wa kumi
na moja wa Yehoramu[o] mwa-
na wa Ahabu kwamba Ahazia[p]
alianza kuwa mfalme juu ya
Yuda.)

30 Mwishowe Yehu akafika
Yezreeli,[q] na Yezebeli[r] akasi-
kia habari hizo. Naye akapa-
ka macho yake wanja[s] na ku-
kipamba kichwa chake,[t] akata-
zama chini kupitia dirishani.[u]
31 Na Yehu akaingia kupitia la-
ngo. Basi yule mwanamke aka-
sema: "Je, mambo yalimwe-
ndea sawa Zimri,[a] aliyemuua
bwana wake?" **32** Basi akai-
nua uso wake kuelekea lile di-
risha na kusema: "Ni nani ali-
ye pamoja nami? Ni nani?"[b]
Mara moja maofisa[c] wawili au
watatu wa makao ya mfalme
wakaangalia chini kumtazama.
33 Basi akasema: "Mwangu-
sheni!"[d] Ndipo wakamwangu-
sha huyo mwanamke, na sehe-
mu ya damu yake ikamwagika
juu ya ukuta na juu ya fara-
si; naye akamkanyaga-kanya-
ga.[e] **34** Kisha akaingia ndani,
akala na kunywa na kisha ku-
sema: "Tafadhali, mshughuliki-
eni mtu huyu aliyelaaniwa[f] na
mkamzike, kwa maana yeye
ni binti ya mfalme."[g] **35** Wa-
lipoenda kumzika, hawakupa-
ta chochote chake isipokuwa
fuvu la kichwa na miguu na vi-
ganja vya mikono.[h] **36** Wali-
porudi na kumwambia, ndipo
akasema: "Hilo ni neno la Ye-
hova alilosema kupitia[i] mtumi-
shi wake Eliya, Mtishbi, kuse-
ma, 'Katika sehemu ya shamba
la Yezreeli mbwa wataila nya-
ma ya Yezebeli.[j] **37** Na maiti
ya Yezebeli itakuwa kama mbo-
lea[k] juu ya uso wa shamba kati-
ka sehemu ya shamba la Ye-
zreeli, ili wasiseme: "Huyu ni
Yezebeli."'"[l]

10 Basi Ahabu alikuwa na
wana 70[m] katika Sama-
ria.[n] Kwa hiyo Yehu akaandi-
ka barua, akazituma Samaria
kwa wakuu[o] wa Yezreeli, wa-
naume wazee[p] na watunzaji wa
Ahabu, na kusema: **2** "Basi,
sasa, wakati ule barua hii ina-
powafikia ninyi, mnao wana wa
bwana wenu pamoja nanyi, na
mnayo magari ya vita na farasi[q]
pamoja nanyi na jiji lenye ngo-
me na silaha. **3** Nanyi mwo-
ne ni nani aliye bora zaidi na

SURA 9
a 1Nya 28:9
Zb 50:22
Mhu 8:13
b 2Fa 7:17
c 2Fa 9:21
d 1Fa 21:29
1Nya 16:12
e Mwa 4:10
Zb 9:12
Zb 72:14
Isa 26:21
f 2Nya 24:25
2Nya 25:4
g Mwa 9:5
Kut 20:5
Law 24:17
Kum 5:9
h 1Fa 21:24
i 2Fa 8:29
2Nya 22:7
j 1Fa 21:2
k Yos 17:11
Amu 1:27
l 1Fa 9:15
m 2Nya 22:7
n 2Sa 5:7
o 2Fa 8:25
p 2Fa 8:24
2Nya 22:2
q 1Fa 21:1
r 1Fa 16:31
1Fa 21:25
s Yer 4:30
Eze 23:40
t Isa 3:18
1Pe 3:3
u Met 7:6

Safu ya 2
a 1Fa 16:16
1Fa 16:18
b Kut 32:26
1Nya 12:18
Zb 94:16
c Mwa 37:36
1Sa 8:15
2Fa 8:6
Est 1:10
d Ayu 31:3
e 2Fa 7:20
Isa 25:10
Mal 4:3
Ro 16:20
f Kum 27:15
Kum 27:25
1Fa 21:25
Zb 119:21
g 1Fa 16:31
h 2Fa 9:10
Isa 14:20
Yer 22:19
i Isa 44:26
Isa 55:11
j 1Fa 21:23
k Zb 83:10
Yer 8:2
Yer 16:4
l Met 10:7

SURA 10
m Amu 8:30
Amu 12:14
n 1Fa 16:29
o Kum 16:18
p 1Fa 21:8
q Met 21:31

mnyoofu zaidi kati ya wana wa bwana wenu, mkamweke yeye juu ya kiti cha ufalme cha baba yake.[a] Halafu mpiganie nyumba ya bwana wenu."

4 Nao wakaogopa sana, wakaanza kusema: "Tazama! Wafalme wawili[b] hawakusimama mbele yake, nasi tutasimamaje?"[c] **5** Kwa hiyo yule aliyekuwa juu ya nyumba na yule aliyekuwa juu ya jiji na wanaume wazee na watunzaji[d] wakatuma ujumbe kwa Yehu, wakisema: "Sisi ni watumishi wako, na kila jambo unalotuambia tutafanya. Hatutamfanya yeyote kuwa mfalme. Fanya yaliyo mema machoni pako."

6 Ndipo akawaandikia barua ya pili, na kusema: "Ikiwa ninyi ni wangu,[e] nanyi mnaitii sauti yangu, chukueni vichwa vya hao wana[f] wa bwana wenu, mje kwangu kesho wakati kama huu katika Yezreeli."[g]

Basi wana wa mfalme, watu 70, walikuwa na wanaume mashuhuri wa jiji waliokuwa wakiwalea. **7** Na ikawa kwamba mara tu barua ile ilipowafikia, wakawachukua wale wana wa mfalme na kuwachinja, watu 70,[h] kisha wakaviweka vichwa vyao ndani ya vikapu, wakampelekea kule Yezreeli. **8** Kisha yule mjumbe[i] akaingia na kumwambia: "Wamevileta vichwa[j] vya wana wa mfalme." Kwa hiyo akasema: "Viwekeni katika mafungu mawili kwenye mwingilio wa lango mpaka asubuhi."[k] **9** Na ikawa kwamba wakati wa asubuhi akaondoka. Kisha akasimama tuli na kuwaambia watu wote: "Ninyi ni waadilifu.[l] Tazama, mimi mwenyewe nilipanga hila[m] juu ya bwana wangu, nami nikamuua;[a] lakini ni nani aliyewapiga na kuwaua hawa wote? **10** Basi jueni kwamba hakuna neno lolote la Yehova litakaloanguka chini[b] bila kutimizwa ambalo Yehova amesema juu ya nyumba ya Ahabu;[c] na Yehova mwenyewe amefanya aliyoyasema kupitia Eliya mtumishi wake."[d] **11** Tena Yehu akaendelea kuwapiga na kuwaua wote waliobaki wa nyumba ya Ahabu katika Yezreeli na watu wake wote walio mashuhuri[e] na rafiki zake na makuhani[f] wake, mpaka alipokuwa amewaangamiza watu wake wote, bila kuacha mwokokaji yeyote abaki.[g]

12 Naye akasimama na kuingia, kisha akaenda zake Samaria. Nyumba ya kufungia ya wachungaji ilikuwa njiani. **13** Na Yehu akakutana na ndugu[h] za Ahazia[i] mfalme wa Yuda. Alipowaambia, "Ninyi ni nani?" ndipo wakasema: "Sisi ni ndugu za Ahazia, nasi tuko njiani kwenda kuuliza kama ni salama kwa wana wa mfalme na kwa wana wa malkia." **14** Mara moja akasema: "Wakamateni wakiwa hai!"[j] Kwa hiyo wakawakamata wakiwa hai, wakawachinja kando ya tangi la maji la ile nyumba ya kufungia, watu 42, naye hakumwacha hata mmoja wao abaki.[k]

15 Alipokuwa akienda kutoka hapo, akakutana na Yehonadabu[l] mwana wa Rekabu[m] akija kumpokea. Alipombariki,[n] akamwambia: "Je, moyo wako ni mnyoofu kunielekea mimi, kama vile moyo wangu ulivyo kuuelekea moyo wako?"[o]

Ndipo Yehonadabu akasema: "Ndiyo."

"Ikiwa ndivyo, nipe mkono wako."

SURA 10
a 2Fa 10:1
b 2Fa 9:24
2Fa 9:27
c Lu 14:31
d 2Fa 10:1
e 2Fa 9:32
f Kum 5:9
Ayu 21:19
Isa 14:21
Ufu 2:23
g 2Fa 9:30
h Amu 9:5
1Fa 21:21
Zb 109:13
i 2Sa 4:10
2Sa 11:19
j 2Sa 20:22
k Kum 21:23
l 1Sa 24:17
m 2Fa 9:14

Safu ya 2
a 2Fa 9:24
b 1Sa 15:29
Isa 14:27
Isa 44:26
Isa 55:11
c 1Fa 21:24
d 1Fa 21:19
1Fa 21:22
2Fa 9:7
2Fa 9:36
e Zb 125:5
Met 13:20
f 1Fa 18:19
1Fa 22:6
2Fa 23:20
g 1Fa 21:21
h 2Nya 22:8
i 2Fa 8:29
2Fa 9:21
2Nya 22:1
j 1Fa 20:18
k 2Nya 22:8
l Yer 35:6
Yer 35:19
m 1Nya 2:55
n Mwa 47:7
Hes 6:23
Ru 2:4
Ro 12:14
o 1Nya 12:17
Met 17:17

Kwa hiyo akampa mkono
wake. Basi akampandisha nda-
ni ya gari pamoja naye.[a]
16 Kisha akasema: "Enda pa-
moja nami, utazame jinsi amba-
vyo sivumilii ushindani[b] wowo-
te kumwelekea Yehova." Nao
wakaendelea kumwendesha
pamoja naye katika gari lake
la vita. **17** Mwishowe akafika
Samaria. Sasa akaanza kuwa-
piga na kuwaua wote waliobaki wa Ahabu katika Samaria,
mpaka akawaangamiza,[c] kulingana na neno la Yehova alilomwambia Eliya.[d]

18 Tena Yehu akakusanya
watu wote na kuwaambia:
"Ahabu alimwabudu Baali kwa
kiwango kidogo tu.[e] Lakini
Yehu atamwabudu kwa kiwa-
ngo kikubwa. **19** Basi sasa
waiteni kwangu manabii[f] wote
wa Baali, waabudu[g] wake wote
na makuhani[h] wake wote. Msi-
ache hata mmoja akose kuwa-
po, kwa sababu nina dhabihu
kubwa kwa ajili ya Baali. Yeyo-
te atakayekosa kuwapo hataen-
delea kuishi." Kwa habari ya
Yehu, yeye alitenda kwa uja-
nja,[i] kusudi awaharibu waabu-
du wa Baali.

20 Na Yehu akaendelea ku-
sema: "Takaseni kusanyiko kuu
kwa ajili ya Baali." Basi waka-
litangaza. **21** Kisha Yehu aka-
tuma ujumbe katika Israeli
yote,[j] hivi kwamba waabudu
wote wa Baali wakaja. Hakuna
hata mmoja aliyebaki ambaye
hakuja. Nao wakaendelea kui-
ngia katika nyumba ya Baali,[k]
na nyumba ya Baali ikajaa ku-
toka mwisho mpaka mwisho.
22 Sasa akamwambia yule ali-
yesimamia chumba cha nguo:
"Toa mavazi kwa ajili ya waa-
budu wote wa Baali." Basi aka-
watolea mavazi. **23** Ndipo
Yehu akaingia na Yehonadabu[a]
mwana wa Rekabu katika nyu-
mba ya Baali. Sasa akawaam-
bia waabudu wa Baali: "Tafu-
teni kwa uangalifu mhakikishe
kwamba hamna hapa ndani pa-
moja nanyi waabudu wowote
wa Yehova, isipokuwa tu waa-
budu wa Baali."[b] **24** Mwisho-
we wakaingia ili kutoa dhabi-
hu na matoleo ya kuteketezwa,
na Yehu akaweka watu 80 upa-
nde wa nje ili wawepo kwa aji-
li yake, naye akaendelea kuse-
ma: "Mtu yeyote atakayeponyo-
ka kati ya watu ninaotia miko-
noni mwenu, nafsi ya huyo mtu
itakuwa badala ya nafsi ya yule
mwingine."[c]

25 Na ikawa kwamba mara
tu alipomaliza kutoa lile to-
leo la kuteketezwa, Yehu aka-
waambia mara moja wale wa-
kimbiaji na maamiri wasaidi-
zi: "Ingieni ndani, wapigeni
na kuwaua! Msiache hata mmo-
ja atoke nje."[d] Na wale wa-
kimbiaji na maamiri wasaidizi[e] wakaanza kuwapiga na ku-
waua kwa makali ya upanga
na kuwatupa nje, nao wakazi-
di kwenda mpaka kwenye jiji
la nyumba ya Baali. **26** Ki-
sha wakazitoa nje nguzo taka-
tifu[f] za nyumba ya Baali na ku-
teketeza[g] kila moja kwa moto.
27 Tena wakabomoa nguzo ta-
katifu ya Baali[h] na kuibomoa
nyumba ya Baali,[i] nao wakaite-
nga iwe choo[j] mpaka leo hii.

28 Kwa hiyo Yehu akaanga-
miza Baali kutoka katika Isra-
eli. **29** Ni dhambi tu za Yero-
boamu[k] mwana wa Nebati, ali-
zosababisha Israeli kutenda
dhambi,[l] ambazo Yehu haku-
geuka asizifuate, yaani, wale
ndama wa dhahabu[m] ambao
mmoja alikuwa katika Bethe-
li na mwingine katika Dani.[n]

SURA 10

a Zek 8:23
b Hes 25:11
1Fa 19:10
c 2Fa 9:8
2Nya 22:7
Zb 58:10
d 1Fa 21:21
2Fa 9:26
Zb 9:16
e 1Fa 16:32
1Fa 18:22
1Fa 18:40
2Fa 3:2
f 2Fa 3:13
g 2Fa 10:21
h 2Fa 10:11
i Met 24:6
Mhu 9:12
j 1Fa 11:35
k 1Fa 16:32

Safu ya 2

a 2Fa 10:15
Yer 35:6
Yer 35:19
b 1Fa 18:22
c 1Fa 20:39
d Kut 32:27
Kum 13:6
Kum 13:8
Eze 9:5
e 2Fa 7:17
2Fa 9:25
f Law 26:1
1Fa 14:23
g Kum 7:25
2Sa 5:21
2Fa 19:18
h Law 26:30
Kum 7:5
i 1Fa 16:32
j Ezr 6:11
Da 2:5
k 1Fa 13:33
l 1Fa 14:16
2Fa 14:24
m 1Fa 12:28
Ho 8:6
n 1Fa 12:29

30 Basi Yehova akamwambia
Yehu: "Kwa kuwa umetenda
vema kwa kufanya yaliyo sawa
machoni pangu,[a] nawe umeite-
ndea nyumba ya Ahabu[b] kuli-
ngana na yote yaliyokuwa mo-
yoni mwangu, wana, kufikia ki-
zazi cha nne, wataketi kwa ajili
yako juu ya kiti cha ufalme cha
Israeli."[c] **31** Na Yehu hakuwa
mwangalifu ili atembee kati-
ka sheria ya Yehova, Mungu wa
Israeli, kwa moyo wake wote.[d]
Yeye hakugeuka kutoka kati-
ka dhambi za Yeroboamu alizo-
sababisha Israeli kutenda dha-
mbi.[e]

32 Siku hizo Yehova akaa-
nza kukatilia mbali Israeli ki-
pande kimoja baada ya kingine;
na Hazaeli[f] akaendelea kuwa-
piga katika eneo lote la Israe-
li, **33** kutoka Yordani kuele-
kea mashariki, nchi yote ya Gi-
leadi,[g] Wagadi[h] na Warubeni[i] na
Wamanase,[j] kutoka Aroeri,[k] li-
liloko kando ya bonde la mto
la Arnoni, naam, Gileadi na Ba-
shani.[l]

34 Na mambo mengine ya
Yehu na yote aliyofanya na
uwezo wake wote, je, hayaku-
andikwa katika kitabu[m] cha
mambo ya siku za wafalme wa
Israeli? **35** Mwishowe Yehu
akalala pamoja na mababu[n]
zake, nao wakamzika katika
Samaria; na Yehoahazi[o] mwa-
na wake akaanza kutawala ma-
hali pake. **36** Na siku ambazo
Yehu alitawala juu ya Israeli zi-
likuwa miaka 28 katika Sama-
ria.

11 Basi kwa habari ya
Athalia[p] mama ya Aha-
zia,[q] yeye aliona kwamba mwa-
na wake amekufa. Kwa hiyo
akasimama, akauangamiza
uzao wote wa ufalme.[r] **2** Hata
hivyo, Yehosheba[s] binti ya Mfa-
lme Yehoramu, dada ya Ahazia,
akamchukua Yehoashi[a] mwa-
na wa Ahazia, akamwiba kuto-
ka kati ya wana wa mfa-
lme waliopaswa kuuawa, naam,
yeye na mlezi wake mwana-
mke, akamwingiza katika chu-
mba cha ndani cha vitanda,
nao wakaendelea kumficha[b]
kutoka machoni pa Athalia,
naye hakuuawa. **3** Naye aka-
endelea kuwa pamoja na mwa-
namke huyo mafichoni kati-
ka nyumba ya Yehova kwa mia-
ka sita, Athalia alipokuwa aki-
tawala juu ya nchi.[c]

4 Na katika mwaka wa saba
Yehoyada[d] akatuma watu, ki-
sha akawachukua wakuu wa
mamia wa walinzi Wakari[e] na
wa wakimbiaji[f] na kuwaleta
kwake katika nyumba ya Ye-
hova, akafanya agano[g] pamo-
ja nao na kuwaapisha[h] katika
nyumba ya Yehova, kisha aka-
waonyesha mwana wa mfalme.
5 Naye akawaamuru, akisema:
"Hivi ndivyo mtakavyofanya:
Sehemu ya tatu kati yenu mtai-
ngia siku ya sabato na kuweka
ulinzi mkali juu ya nyumba ya
mfalme;[i] **6** na sehemu ya tatu
watakuwa kwenye Lango[j] la
Msingi, na sehemu ya tatu wa-
takuwa katika lango nyuma ya
wakimbiaji; nanyi mweke uli-
nzi mkali juu ya nyumba[k] kwa
zamu. **7** Na kuna migawanyo
miwili kati yenu ambayo yote
inatoka siku ya sabato, nao la-
zima waweke ulinzi mkali juu
ya nyumba ya Yehova kwa aji-
li ya mfalme. **8** Nanyi mnapa-
swa kumzunguka mfalme pa-
nde zote, kila mmoja akiwa na
silaha zake mkononi mwake;
na yeyote atakayeingia katikati
ya vikosi atauawa. Nanyi mwe-
ndelee kuwa na mfalme anapo-
toka nje na anapoingia ndani."

SURA 10

a Eze 29:20
b 1Fa 21:21
c 2Fa 13:1
2Fa 13:10
2Fa 14:23
2Fa 15:8
2Fa 15:12
Ayu 34:11
Ebr 6:10
d Kum 10:12
1Fa 2:4
Zb 78:10
Met 4:23
Ho 1:4
Ebr 10:38
e 1Fa 12:30
1Fa 13:34
1Fa 14:16
f 1Fa 19:17
2Fa 8:12
2Fa 13:22
Amo 1:4
g Kum 3:15
Yos 22:9
h Kum 3:16
i Hes 32:33
j Kum 3:13
k Yos 13:9
l Kum 28:63
Yos 13:12
m 1Fa 14:19
2Fa 13:8
n 2Sa 7:12
o 2Fa 13:1
2Fa 13:7

SURA 11

p 2Fa 8:26
2Fa 11:20
2Nya 21:6
2Nya 22:10
2Nya 24:7
q 2Fa 9:27
2Nya 22:1
r 2Nya 21:4
Ro 1:29
s 2Nya 22:11

Safu ya 2

a 2Fa 12:1
b Amu 9:5
2Fa 8:19
Zb 27:5
c 2Nya 22:12
Zb 12:8
Isa 3:12
Mal 3:15
1Ti 2:12
d 2Fa 11:9
2Nya 23:1
e 2Fa 11:15
2Fa 11:19
f 1Sa 8:11
1Sa 22:17
2Sa 18:19
1Fa 14:27
g 1Sa 18:3
2Fa 23:3
2Nya 15:12
h Kum 6:13
Yer 12:16
Ebr 6:16
i 1Fa 7:1
j 2Nya 23:5
k 1Fa 6:1

9 Na wale wakuu wa mamia[a] wakafanya kulingana na yote ambayo Yehoyada kuhani alikuwa ameamuru. Basi kila mmoja wao akachukua watu wake waliokuwa wakiingia wakati wa sabato,[b] pamoja na wale waliokuwa wakitoka nje wakati wa sabato, kisha wakamjia Yehoyada kuhani. **10** Sasa kuhani akawapa wale wakuu wa mamia mikuki na ngao za mviringo zilizokuwa za Mfalme Daudi, ambazo zilikuwa katika nyumba ya Yehova.[c] **11** Na wakimbiaji[d] wakaendelea kusimama kila mmoja akiwa na silaha zake mkononi mwake, kuanzia upande wa kuume wa nyumba mpaka upande wa kushoto wa nyumba, kando ya madhabahu[e] na kando ya nyumba, pande zote karibu na mfalme. **12** Kisha akamtoa nje mwana[f] wa mfalme, akamvika taji[g] na ule Ushuhuda;[h] na basi wakamfanya kuwa mfalme[i] na kumtia mafuta.[j] Nao wakaanza kupiga makofi[k] na kusema: "Mfalme na aishi!"[l]

13 Athalia aliposikia sauti ya watu wakikimbia, mara moja akaingia kwa watu katika nyumba ya Yehova.[m] **14** Kisha akaona, na tazama, mfalme alikuwa amesimama kando ya nguzo[n] kama ilivyo desturi, na wakuu na tarumbeta[o] kando ya mfalme, na watu wote wa nchi wakishangilia[p] na kupiga tarumbeta. Athalia[q] akayararua mavazi yake mara moja, akaanza kulia: "Ni hila! Ni hila!"[r] **15** Lakini Yehoyada kuhani akawaamuru wakuu wa mamia, watu waliochaguliwa wa jeshi,[s] na kuwaambia: "Mwondoeni katikati ya vikosi, na yeyote atakayemfuata, auawe kwa upanga!"[t] Kwa maana kuhani yule alikuwa amesema: "Asiuawe ndani ya nyumba ya Yehova." **16** Basi wakamkamata, akafika kando ya njia ya mlango wa farasi[a] wa nyumba ya mfalme,[b] naye akauawa huko.[c]

17 Ndipo Yehoyada akafanya agano[d] kati ya Yehova[e] na mfalme[f] na watu, ili kwamba wajionyeshe kuwa watu wa Yehova; na pia kati ya mfalme na watu.[g] **18** Kisha watu wote wa nchi wakaenda kwenye nyumba ya Baali, wakazibomoa madhabahu zake;[h] nao wakazivunja kabisa[i] sanamu zake, nao, mbele ya zile madhabahu,[j] wakamuua Matani[k] kuhani wa Baali.

Na kuhani akaweka waangalizi juu ya nyumba ya Yehova.[l] **19** Tena akawachukua wakuu wa mamia na walinzi Wakari[m] na wakimbiaji[n] na watu wote wa nchi, ili wamshushe mfalme kutoka katika nyumba ya Yehova; nao wakaja polepole kupitia njia ya lango[o] la wakimbiaji mpaka kwenye nyumba ya mfalme; naye akaanza kuketi juu ya kiti cha wafalme.[p] **20** Na watu wote wa nchi wakaendelea kushangilia;[q] nalo jiji halikuwa na usumbufu, nao walikuwa wamemuua Athalia kwa upanga nyumbani kwa mfalme.[r]

21 Yehoashi[s] alikuwa na umri wa miaka saba alipoanza kutawala.[t]

12 Katika mwaka wa 7 wa Yehu,[u] Yehoashi[v] akawa mfalme, naye akatawala miaka 40 katika Yerusalemu. Na jina la mama yake lilikuwa Sibia kutoka Beer-sheba. **2** Na Yehoashi akaendelea kufanya yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova siku zake zote ambazo Yehoyada kuhani alimfundi-

SURA 11

a 2Fa 11:4
b 2Nya 23:8
c 2Nya 23:9
d 1Sa 8:11
2Sa 15:1
1Fa 14:27
e Kut 40:6
1Fa 8:22
2Nya 4:1
f 2Fa 11:2
2Nya 23:11
g 2Sa 1:10
Zb 132:18
h Kut 25:21
Kut 31:18
i 1Fa 1:38
j Kut 30:23
1Fa 1:39
k 1Fa 1:40
Zb 47:1
l 1Fa 1:34
Zb 72:15
Mhu 10:17
m 2Nya 23:12
n 2Fa 23:3
2Nya 34:31
o 2Nya 5:12
p 1Fa 1:40
Met 29:2
q 2Fa 11:1
2Fa 11:3
r 2Nya 23:13
s 2Fa 11:4
2Nya 23:9
t 2Nya 23:14

Safu ya 2

a 2Nya 23:15
b 1Fa 7:1
c Mwa 9:6
Kut 21:12
Law 24:17
Hes 35:30
d Yos 24:25
e Kum 5:3
f 1Sa 10:25
2Sa 5:3
g 2Nya 23:16
h Kum 12:3
i Kum 7:25
j Kum 13:5
Kum 13:9
k 2Nya 23:17
l 2Nya 23:18
m 2Fa 11:4
2Fa 11:15
n 1Fa 14:27
o 2Nya 23:20
p 2Sa 7:16
1Nya 29:23
Yer 17:25
Yer 22:4
q Met 11:10
Met 29:2
r 2Nya 23:21
s 2Fa 11:2
t 2Nya 24:1

SURA 12

u 1Fa 19:16
2Fa 10:30
v 2Fa 11:2
1Nya 3:11
2Nya 24:1

sha.[a] **3** Ni mahali pa juu peke
yake ndipo hapakuondolewa.[b]
Watu walikuwa wangali wana-
toa dhabihu na kufukiza moshi
wa dhabihu katika mahali pa
juu.

4 Na Yehoashi akawaambia
makuhani:[c] "Pesa zote kwa ajili
ya matoleo[d] matakatifu zinazo-
letwa katika nyumba ya Yeho-
va,[e] pesa ambazo kila mtu hu-
kadiriwa,[f] pesa kwa ajili ya
nafsi kulingana na kadirio la
thamani[g] ya mtu mmoja-
mmoja, pesa zote ambazo kila
mmoja anaazimia moyoni ku-
leta nyumbani kwa Yehova,[h]
5 makuhani na wazichukue,
kila mmoja kutoka kwa mtu
wanayefahamiana naye;[i] nao
warekebishe mipasuko ya nyu-
mba popote panapopatikana
mpasuko wowote."[j]

6 Na ikawa kwamba kufikia
mwaka wa 23 wa Mfalme Yeho-
ashi, makuhani hawakuwa wa-
merekebisha mipasuko ya nyu-
mba.[k] **7** Kwa hiyo Mfalme Ye-
hoashi akamwita Yehoyada[l]
kuhani na makuhani, akawaam-
bia: "Kwa nini hamrekebi-
shi mipasuko ya nyumba? Basi
sasa, msichukue pesa zaidi ku-
toka kwa watu mnaofahamia-
na nao, bali mzitoe kwa aji-
li ya mipasuko ya nyumba."[m]
8 Ndipo makuhani wakakuba-
li wasichukue pesa zaidi kuto-
ka kwa watu na kutorekebisha
mipasuko ya nyumba.

9 Basi Yehoyada kuhani aka-
chukua sanduku,[n] akatoboa
tundu katika kifuniko chake,
akaliweka kando ya madha-
bahu upande wa kuume mtu
anapoingia ndani ya nyumba
ya Yehova, na makuhani, watu-
nza-malango,[o] wakaweka humo
pesa[p] zote zilizokuwa zikile-
twa katika nyumba ya Yehova.

SURA 12

a 2Fa 14:3
2Nya 24:2
b Hes 33:52
Yer 2:20
c Kut 28:1
2Nya 35:2
d 1Nya 18:11
2Nya 31:12
e 1Fa 7:51
f Kut 30:13
2Nya 24:9
g Law 27:2
Law 27:12
h Kut 25:2
Kut 35:21
Ne 10:39
2Ko 9:11
i Hes 18:8
Hes 18:28
j 2Nya 24:7
k 2Nya 24:5
Ro 12:11
Kol 3:23
l 2Fa 11:4
2Nya 23:1
2Nya 24:15
m 2Nya 24:6
n 2Nya 24:8
Mk 12:41
Lu 21:1
o 2Fa 11:6
Zb 84:10
p 2Nya 24:10
Mt 6:4
2Ko 9:7

Safu ya 2

a 2Sa 20:25
2Fa 18:18
b 2Nya 24:11
c 2Fa 22:5
2Nya 24:12
2Nya 34:10
d 1Fa 5:17
Ezr 5:8
e 1Fa 7:50
f 2Nya 4:22
g Hes 10:2
2Nya 5:12
h 2Nya 24:14
i 2Nya 24:13
j 2Fa 22:7
k 2Nya 34:12
l 1Ko 4:2
m Law 5:15
Law 7:7
n Hes 18:8
o 1Fa 19:15
2Fa 8:13
2Fa 10:32
Amo 1:4
p 1Nya 18:1

10 Na ikawa kwamba mara tu
walipoona kuna pesa nyingi
sana katika lile sanduku, mwa-
ndishi[a] wa mfalme na kuhani
mkuu wakawa wakija, nao wa-
kazifunga na kuhesabu pesa zi-
lizokuwa zikipatikana kwenye
nyumba ya Yehova.[b] **11** Na
zile pesa ambazo zilikuwa zime-
hesabiwa, wakaziweka mikono-
ni mwa wafanyakazi[c] waliowe-
kwa kwenye nyumba ya Yeho-
va. Wao nao wakazilipa kwa
wafanyakazi wa mbao na kwa
wajenzi waliokuwa wakifanya
kazi katika nyumba ya Yehova,
12 na kwa waashi na kwa wa-
chongaji wa mawe,[d] na kwa aji-
li ya kununua mbao na mawe
yaliyochongwa kwa ajili ya ku-
rekebisha mipasuko ya nyumba
ya Yehova na kwa ajili ya vyote
vilivyotumiwa kwenye nyumba
ili kuirekebisha.

13 Ila tu kuhusiana na nyu-
mba ya Yehova hawakutenge-
neza beseni za fedha, mikasi
ya taa,[e] mabakuli,[f] tarumbeta,[g]
chombo chochote cha dhahabu
na chombo cha fedha kutokana
na zile pesa zilizokuwa zikile-
twa katika nyumba ya Yehova;[h]
14 kwa maana walikuwa wa-
kiwapa wale wafanyakazi, nao
walizitumia kurekebisha nyu-
mba ya Yehova.[i] **15** Nao ha-
wakuwa wakitoza hesabu[j] wale
watu ambao mkononi mwao
pesa zilitiwa ili kuwapa wale
wafanyakazi,[k] kwa sababu wa-
likuwa wakifanya kazi kwa ua-
minifu.[l] **16** Na pesa za mato-
leo ya hatia[m] na pesa za matoleo
ya dhambi, hazikuwa zikiletwa
katika nyumba ya Yehova. Kwa
hiyo zikawa za makuhani.[n]

17 Ndipo ikawa kwamba Ha-
zaeli[o] mfalme wa Siria akapa-
nda kwenda kupigana na Ga-
thi,[p] akaliteka, kisha Hazaeli

akaelekeza uso[a] wake apande
kwenda juu ya Yerusalemu.[b]
18 Kwa hiyo Yehoashi mfa-
lme wa Yuda akachukua ma-
toleo yote matakatifu[c] amba-
yo Yehoshafati na Yehoramu
na Ahazia mababu zake, wafa-
lme wa Yuda, walikuwa wame-
yatakasa na matoleo yake mwe-
nyewe matakatifu na dhahabu
yote iliyoonekana katika hazi-
na za nyumba ya Yehova na
nyumba ya mfalme, akavipeleka[d]
kwa Hazaeli mfalme wa Si-
ria. Basi akaondoka juu ya Ye-
rusalemu.

19 Na mambo mengine ya
Yehoashi na yote aliyoyafanya,
je, hayakuandikwa katika kita-
bu[e] cha mambo ya siku za wafa-
lme wa Yuda? **20** Hata hivyo,
watumishi[f] wake wakasimama
na kuungana katika hila,[g] wa-
kampiga na kumuua Yehoashi
katika nyumba[h] ya Kilima,[i] ka-
tika njia inayoshuka kwenda
Sila. **21** Na Yozakari mwana
wa Shimeathi na Yehozabadi[j]
mwana wa Shomeri, watumishi
wake, ndio waliompiga, hata
akafa. Basi wakamzika pamo-
ja na mababu zake katika Jiji
la Daudi; na Amazia[k] mwana
wake akaanza kutawala maha-
li pake.

13 Katika mwaka wa 23 wa
Yehoashi[l] mwana wa
Ahazia[m] mfalme wa Yuda, Ye-
hoahazi[n] mwana wa Yehu[o] aka-
wa mfalme juu ya Israeli
katika Samaria kwa miaka 17.
2 Naye akaendelea kufanya ya-
liyokuwa mabaya machoni pa
Yehova,[p] akaifuatilia dhambi ya
Yeroboamu[q] mwana wa Nebati,
aliyosababisha Israeli kutenda
dhambi.[r] Hakugeuka aiache.
3 Na hasira[s] ya Yehova ikawa-
ka juu ya Israeli, hivi kwamba
akawatia mkononi mwa Hazae-
li[a] mfalme wa Siria na mkono-
ni mwa Ben-hadadi[b] mwana wa
Hazaeli siku zao zote.

4 Baada ya muda Yehoahazi
akautuliza[c] uso wa Yehova, hata
Yehova akamsikiliza;[d] kwa ma-
ana alikuwa ameona kukanda-
mizwa kwa Israeli,[e] kwa sababu
mfalme wa Siria alikuwa ame-
wakandamiza.[f] **5** Basi Yeho-
va akawapa Israeli mwokozi,[g]
hata wakatoka chini ya mko-
no wa Siria, na wana wa Israeli
wakaendelea kukaa katika nyu-
mba zao kama hapo mwanzo-
ni.[h] **6** (Isipokuwa tu hawakua-
cha dhambi ya nyumba ya Ye-
roboamu, aliyosababisha Israeli
watende dhambi.[i] Alitembea ka-
tika hiyo;[j] na hata mti mtakatifu[k] ulisimama katika Samaria.)
7 Kwa maana hakuwa ame-
mwachia Yehoahazi watu wo-
wote isipokuwa wapanda-farasi 50 na magari 10 na watu
10,000 wanaoenda kwa miguu,[l]
kwa sababu mfalme wa Siria ali-
kuwa amewaharibu,[m] ili awafa-
nye kuwa kama mavumbi waka-
ti wa kupura.[n]

8 Na mambo mengine ya Ye-
hoahazi na yote aliyoyafanya
na uwezo wake, je, hayakuandi-
kwa katika kitabu[o] cha mambo
ya siku za wafalme wa Israeli?
9 Mwishowe Yehoahazi akala-
la pamoja na mababu zake, nao
wakamzika katika Samaria;[p] na
Yehoashi[q] mwana wake akaa-
nza kutawala mahali pake.

10 Katika mwaka wa 37 wa
Yehoashi mfalme wa Yuda, Ye-
hoashi[r] mwana wa Yehoaha-
zi akawa mfalme juu ya Israeli
katika Samaria kwa miaka 16.
11 Naye akaendelea kutenda
yaliyokuwa mabaya machoni
pa Yehova.[s] Hakuziacha dha-
mbi zote za Yeroboamu mwana
wa Nebati, alizosababisha Isra-

SURA 12
a Yer 42:15
Lu 9:51
b 2Nya 24:23
c 1Fa 15:18
d 2Fa 16:8
2Fa 18:15
e 1Fa 14:29
2Fa 8:23
f 2Fa 14:5
g 2Nya 24:25
2Nya 25:27
h 1Fa 9:15
i 2Sa 5:9
1Fa 9:24
1Fa 11:27
2Nya 32:5
j 2Nya 24:26
k 2Nya 24:27

SURA 13
l 2Fa 11:2
2Fa 11:21
m 2Fa 8:26
2Fa 9:27
n 2Fa 10:35
o 2Fa 10:30
p Kum 28:15
q 1Fa 12:28
1Fa 13:33
r 1Fa 14:16
s Law 26:17
Kum 6:15
Kum 7:4
Zb 7:11
Ebr 12:29

Safu ya 2
a 1Fa 19:17
2Fa 8:12
b 2Fa 13:24
c Amu 6:6
Amu 10:10
2Nya 33:13
Zb 78:34
d Kum 4:7
Zb 50:15
Zb 65:2
1Yo 5:14
e Mwa 31:42
Kut 3:7
Amu 10:16
f 2Fa 14:26
g Ne 9:27
h Zb 130:4
i 2Fa 10:29
2Fa 17:21
j 1Fa 16:26
k Kum 7:5
1Fa 14:15
1Fa 16:33
l 2Fa 10:32
m Kum 28:45
2Fa 8:12
n Amo 1:3
o 1Fa 14:19
2Fa 10:34
p 2Fa 10:35
q 2Fa 14:8
r 2Fa 14:1
s 2Fa 13:2
Ho 5:11

eli kutenda dhambi.[a] Alitembea
katika hizo.
12 Na mambo mengine ya
Yehoashi na yote aliyoyafa-
nya na uwezo wake na jinsi ali-
vyopigana[b] na Amazia mfa-
lme wa Yuda, je, hayakuandi-
kwa katika kitabu[c] cha mambo
ya siku za wafalme wa Israeli?
13 Mwishowe Yehoashi akala-
la pamoja na mababu zake, na
Yeroboamu[d] akaketi juu ya kiti
chake cha ufalme. Naye Yeho-
shi akazikwa katika Samaria
pamoja na wafalme wa Israeli.[e]
14 Naye Elisha[f] alikuwa
ameshikwa na ugonjwa ambao
ulikuwa wa kumuua.[g] Basi Ye-
hoashi mfalme wa Israeli aka-
shuka kuja kwake, akaanza ku-
lia juu ya uso wake, akisema:
"Baba yangu,[h] baba yangu, gari
la vita la Israeli na wapanda-fa-
rasi wake!"[i] **15** Na Elisha
akamwambia: "Chukua upinde
na mishale." Basi akachukua
upinde na mishale. **16** Naye
akaendelea kumwambia mfa-
lme wa Israeli: "Weka mkono
kwenye upinde." Basi akawe-
ka mkono wake kwenye upinde,
halafu Elisha akaweka mikono
yake juu ya mikono[j] ya mfalme.
17 Ndipo akasema: "Fungua di-
risha la upande wa mashariki."
Basi akalifungua. Mwishowe
Elisha akasema: "Piga!" Basi
akapiga. Sasa akasema: "Msha-
le wa wokovu wa Yehova, naam,
mshale wa wokovu[k] juu ya Si-
ria! Nawe hakika utaipiga Siria
kule Afeki[l] kufikia hatua ya ku-
imaliza."
18 Naye akaendelea kuse-
ma: "Chukua mishale." Basi
akaichukua. Kisha akamwa-
mbia mfalme wa Israeli: "Piga
chini." Basi akapiga mara tatu
halafu akaacha.[m] **19** Na yule
mtu wa Mungu wa kweli[n] aka-

SURA 13
a 2Fa 10:29
b 2Fa 14:8
2Fa 14:13
2Nya 25:17
c 1Fa 14:19
2Fa 10:34
d 2Fa 14:28
e 2Fa 10:35
2Fa 13:9
f 1Fa 19:16
2Fa 5:8
g Zek 1:5
h 2Fa 5:13
i 2Fa 2:12
j Zb 144:1
k Zb 18:14
l 1Sa 29:1
1Fa 20:26
m Ga 6:9
n Isa 44:26

Safu ya 2
a 2Fa 13:25
b Zb 139:8
c 2Fa 24:2
d 2Fa 1:1
e Yoh 11:44
Ebr 11:35
f Ufu 11:11
g 1Fa 19:15
2Fa 10:32
h 2Fa 8:12
Zb 106:41
i Amu 10:16
2Fa 14:27
Ne 9:31
Zb 86:15
Isa 30:18
Omb 3:32
j Zb 145:8
2Ko 1:3
Efe 2:4
k Kut 2:24
l Mwa 13:16
Mwa 17:7
Mwa 22:17
Kut 32:13
m Mwa 26:3
n Mwa 28:13
Law 26:42
o Zb 105:8
Mik 7:20
Ebr 6:18
p 2Fa 13:19

SURA 14
q 2Fa 13:10
r 1Nya 3:12

mkasirikia; kwa hiyo akasema:
"Ilikupasa upige mara tano au
mara sita! Kama ingekuwa hi-
vyo, ungeipiga Siria kufikia ha-
tua ya kuimaliza, lakini sasa
utaipiga Siria mara tatu."[a]
20 Kisha Elisha akafa, nao
wakamzika.[b] Na palikuwa na
vikundi vya waporaji[c] vya Wa-
moabu[d] waliokuja kwa uka-
waida katika nchi mwanzo-
ni mwa mwaka. **21** Na ikawa
kwamba walipokuwa wakimzi-
ka mtu, tazama, wakaona ki-
kundi cha waporaji. Wakamtu-
pa mara moja yule mtu ndani
ya kaburi la Elisha, wakaenda
zao. Mtu yule alipoigusa mifu-
pa ya Elisha, akawa hai[e] mara
moja na kusimama kwa miguu[f]
yake.
22 Kwa habari ya Hazaeli[g]
mfalme wa Siria, yeye aliwaka-
ndamiza[h] Israeli siku zote za Ye-
hoahazi. **23** Hata hivyo, Ye-
hova akawapa kibali[i] na kuwa-
onea rehema[j] na kuwageukia
kwa ajili ya agano[k] lake na
Abrahamu,[l] Isaka[m] na Yakobo;[n]
naye hakutaka kuwaangami-
za,[o] wala hakuwatupilia mbali
kutoka mbele za uso wake mpa-
ka sasa. **24** Mwishowe Hazae-
li mfalme wa Siria akafa, na
Ben-hadadi mwana wake aka-
anza kutawala mahali pake.
25 Na Yehoashi mwana wa Ye-
hoahazi akachukua tena kuto-
ka mkononi mwa Ben-hada-
di mwana wa Hazaeli yale ma-
jiji aliyokuwa amechukua ku-
toka mkononi mwa Yehoahazi
baba yake katika vita. Yehoashi
akampiga mara tatu, naye aka-
yarudisha majiji ya Israeli.[p]

14 Katika mwaka wa pili
wa Yehoashi[q] mwana wa
Yehoahazi mfalme wa Israe-
li, Amazia[r] mwana wa Yeho-
ashi mfalme wa Yuda, akawa

mfalme. **2** Alikuwa na umri
wa miaka 25 alipoanza kuta-
wala, naye akatawala miaka 29
katika Yerusalemu. Na jina la
mama yake lilikuwa Yehoadi-
ni[a] wa Yerusalemu. **3** Naye
akaendelea kufanya yaliyoku-
wa manyoofu machoni pa Yeho-
va,[b] ila tu si kama Daudi babu
yake.[c] Akafanya kulingana na
yote ambayo Yehoashi baba
yake alifanya.[d] **4** Ni mahali
pa juu peke yake ndipo hapa-
kuondolewa.[e] Watu walikuwa
bado wanatoa dhabihu na ku-
fukiza moshi wa dhabihu kati-
ka mahali pa juu.[f] **5** Na ika-
wa kwamba mara tu ufalme
ulipokuwa umeimarishwa mko-
noni mwake, akaanza kuwapi-
ga na kuwaua[g] wale watumishi
wake waliompiga na kumuua
mfalme, baba yake.[h] **6** Naye
hakuwaua wana wa wale wali-
ompiga na kumuua, kulinga-
na na yale ambayo yameandi-
kwa katika kitabu cha sheria
ya Musa ambayo Yehova alia-
muru, akisema:[i] "Akina baba
wasiuawe kwa sababu ya wana,
na wana wasiuawe kwa sababu
ya akina baba; bali kila mmo-
ja auawe kwa sababu ya dhambi
yake mwenyewe."[j] **7** Yeye ali-
wapiga na kuwaua Waedomu[k]
katika Bonde la Chumvi,[l] watu
elfu kumi, akateka Sela katika
vita hivyo, na jina lake likaitwa
Yoktheeli mpaka leo hii.

8 Kisha wakati huo Amazia
aliwatuma wajumbe kwa Ye-
hoashi mwana wa Yehoaha-
zi mwana wa Yehu mfalme wa
Israeli, na kusema: "Haya njoo.
Tutazamane uso kwa uso."[m]
9 Ndipo Yehoashi mfalme wa
Israeli akatuma ujumbe kwa
Amazia mfalme wa Yuda, na
kusema: "Gugu lenye miiba lili-
lokuwa katika Lebanoni lilitu-
ma ujumbe kwa mwerezi[a] uliokuwa katika Lebanoni, na kusema, 'Mpe mwanangu binti yako awe mke wake.' Hata hivyo, mnyama wa mwituni aliyekuwa katika Lebanoni akapita karibu, akalikanyaga lile gugu lenye miiba.[b] **10** Bila shaka umepiga[c] Edomu, na moyo wako umekuinua.[d] Furahia heshima[e] yako na ukae nyumbani kwako mwenyewe. Kwa nini, basi, ujiingize katika mzozo[f] chini ya hali zisizofaa[g] hata uanguke, wewe na Yuda pamoja nawe?" **11** Na Amazia hakusikiliza.[h]

Basi Yehoashi mfalme wa Israeli akapanda, nao wakatazamana uso kwa uso,[i] yeye na Amazia mfalme wa Yuda, kule Beth-shemeshi,[j] ya Yuda. **12** Na Yuda wakashindwa mbele ya Israeli,[k] hata wakaanza kukimbia, kila mmoja kwenda katika hema lake. **13** Naye Yehoashi mfalme wa Israeli akamkamata Amazia mfalme wa Yuda mwana wa Yehoashi mwana wa Ahazia kule Beth-shemeshi, kisha wakaja Yerusalemu, naye akabomoa shimo katika ukuta wa Yerusalemu katika Lango la Efraimu[l] mpaka kwenye Lango la Pembeni,[m] urefu wa mikono mia nne. **14** Naye akachukua dhahabu yote na fedha na vyombo vyote vilivyopatikana katika nyumba ya Yehova[n] na katika hazina za nyumba ya mfalme na mateka, kisha akarudi Samaria.

15 Na mambo mengine ya Yehoashi, yale aliyoyafanya na uwezo wake na jinsi alivyopigana na Amazia mfalme wa Yuda, je, hayakuandikwa katika kitabu[o] cha mambo ya siku za wafalme wa Israeli? **16** Mwishowe Yehoashi akalala pamoja na

SURA 14

a 2Nya 25:1
b 2Nya 25:2
c 1Fa 15:5
d 2Nya 24:2
2Nya 24:18
Zek 1:4
e 1Fa 15:14
2Fa 12:3
f 2Fa 15:4
2Fa 15:35
g Mwa 9:6
Kut 21:12
Law 24:17
Hes 35:33
h 2Fa 12:20
2Nya 24:25
2Nya 25:3
i 2Nya 25:4
j Kum 24:16
Eze 18:20
k 2Fa 8:20
2Nya 25:11
l 2Sa 8:13
1Nya 18:12
Zb 60:Uta
m 2Sa 2:14
2Nya 25:17
Met 13:10
Met 18:6

Safu ya 2

a Amu 9:15
b 2Nya 25:18
c 2Fa 14:7
d 2Nya 26:16
Met 16:18
Hab 2:4
Ga 6:3
Yak 4:6
e 1Sa 18:8
f 2Nya 35:21
Met 3:30
Met 20:3
g Lu 14:31
h 2Nya 25:16
2Nya 25:20
i 2Nya 25:21
j Yos 15:10
Yos 21:16
1Sa 6:9
1Nya 6:59
k 2Nya 25:22
Met 16:18
l 2Nya 25:23
Ne 8:16
Ne 12:39
m Yer 31:38
Zek 14:10
n 2Fa 12:13
o 1Fa 14:19
2Fa 13:12

mababu zake,[a] akazikwa katika Samaria[b] pamoja na wafalme wa Israeli, na Yeroboamu[c] mwana wake akaanza kutawala mahali pake.

17 Na Amazia[d] mwana wa Yehoashi mfalme wa Yuda akaendelea kuishi kwa miaka kumi na mitano[e] baada ya kifo cha Yehoashi[f] mwana wa Yehoahazi mfalme wa Israeli. **18** Na mambo mengine ya Amazia, je, hayakuandikwa katika kitabu[g] cha mambo ya siku za wafalme wa Yuda?[h] **19** Baadaye wakaungana katika hila[i] juu yake katika Yerusalemu, naye akakimbilia Lakishi;[j] lakini wakatuma watu kumfuatilia huko Lakishi, wakamuua huko.[k] **20** Kwa hiyo wakambeba juu ya farasi, naye akazikwa[l] katika Yerusalemu pamoja na mababu zake katika Jiji la Daudi.[m] **21** Ndipo watu wote wa Yuda wakamchukua Azaria,[n] wakati huo akiwa na umri wa miaka kumi na sita,[o] nao wakamfanya kuwa mfalme mahali pa Amazia[p] baba yake. **22** Yeye alijenga Elathi[q] na kulirudisha kwa Yuda baada ya mfalme kulala pamoja na mababu zake.

18 Naye malaika wa Yehova akamwambia Gadi[r] amwambie Daudi apande kwenda kumsimamishia Yehova madhabahu kwenye uwanja wa kupuria wa Ornani Myebusi.[a] **19** Basi Daudi akapanda kulingana na neno la Gadi ambalo alikuwa amesema katika jina la Yehova.[b] **20** Na wakati huo, Ornani[c] akageuka, akamwona yule malaika; na wanawe wanne waliokuwa pamoja naye walikuwa wamejificha. Sasa Ornani alikuwa akipura ngano. **21** Na Daudi akaja mpaka kwa Ornani. Ornani alipotazama na kumwona Daudi,[d] akatoka haraka nje ya uwanja wa kupuria, akamwinamia Daudi kifudifudi. **22** Ndipo Daudi akamwambia Ornani: "Nipe mahali pa uwanja wa kupuria, ili nimjengee Yehova madhabahu hapo. Unipe kwa pesa kamili,[e] ili tauni[f] ikomeshwe juu ya watu." **23** Lakini Ornani akamwambia Daudi: "Uchukue uwe wako,[g] na bwana wangu mfalme afanye lililo jema machoni pake mwenyewe. Tazama, natoa ng'ombe[h] kwa ajili ya matoleo ya kuteketezwa na chombo cha kupuria[i] kwa ajili ya kuni[j] na ngano kuwa toleo la nafaka. Natoa vyote."[k]

24 Hata hivyo, Mfalme Daudi akamwambia Ornani: "Hapana, bali bila shaka nitaununua kwa pesa kamili,[l] kwa sababu sitachukua kilicho chako nimpe Yehova ili kutoa matoleo ya kuteketezwa bila gharama." **25** Kwa hiyo Daudi akampa Ornani kwa ajili ya mahali hapo shekeli za dhahabu zenye uzito wa mia sita.[m] **26** Ndipo Daudi akamjengea Yehova madhabahu[n] hapo na kutoa dhabihu za kuteketezwa na dhabihu za ushirika, naye akamwitia Yehova,[o]ambaye sasa alimji-

SURA 21
a 2Sa 24:14
b Kut 34:6
Zb 51:1
Isa 55:7
Omb 3:22
c 2Nya 28:9
d Hes 16:46
e 2Sa 24:15
f 2Sa 24:16
g Kut 32:14
Kum 32:36
h Zb 90:13
i 2Sa 24:18
2Nya 3:1
j 2Sa 5:6
k Hes 22:31
l Yos 5:13
m 1Fa 21:27
2Fa 19:1
Zb 35:13
n Hes 16:22
o 2Sa 24:17
Zb 51:4
p Zb 44:11
q Kut 32:12
r 2Sa 24:11

Safu ya 2
a 2Sa 24:18
2Nya 3:1
b 2Sa 24:19
c 1Nya 21:15
d 2Sa 24:20
e Mwa 23:9
2Sa 24:21
f Hes 25:8
g Mwa 23:11
h 1Sa 6:14
1Fa 19:21
i Isa 28:27
j 2Sa 24:22
k 2Sa 24:23
l Mwa 23:13
m 2Sa 24:24
n Kut 20:25
2Sa 24:25
o 1Sa 7:9
Zb 91:15

bu kwa moto[a] kutoka mbinguni
juu ya madhabahu ya toleo la
kuteketezwa. **27** Tena, Yeho-
va akampa amri yule malaika,[b]
naye akarudisha upanga kati-
ka ala yake. **28** Wakati huo,
Daudi alipoona kwamba Yeho-
va amemjibu kwenye uwanja
wa kupuria wa Ornani Myebusi,
yeye akaendelea kutoa dhabihu
hapo.[c] **29** Lakini ile maskani
ya Yehova ambayo Musa aliku-
wa ameitengeneza katika nyi-
ka na ile madhabahu ya toleo
la kuteketezwa, vilikuwa wa-
kati huo katika mahali pa juu
kule Gibeoni.[d] **30** Na Daudi
alikuwa hajaweza kwenda mbe-
le yake ili kutafuta shauri kwa
Mungu, kwa maana alikuwa
ameogopa[e] kwa sababu ya upa-
nga wa malaika wa Yehova.

22 Ndipo Daudi akasema:
"Hii ndiyo nyumba[f] ya Ye-
hova, Mungu wa kweli, na hii
ndiyo madhabahu[g] kwa ajili ya
toleo la kuteketezwa kwa ajili
ya Israeli."

2 Sasa Daudi akasema wa-
kaaji wote wageni[h] walio kati-
ka nchi ya Israeli wakusanywe,
kisha akawaweka kuwa wacho-
ngaji wa mawe[i] ili wachonge
mawe ya mraba[j] kwa ajili ya
kujenga nyumba ya Mungu wa
kweli. **3** Na Daudi akatayari-
sha chuma kwa wingi sana kwa
ajili ya misumari ya milango ya
malango na kwa ajili ya viba-
nio, na pia shaba nyingi isi-
yoweza kupimwa uzito,[k] **4** na
pia mbao za mierezi[l] zisizo na
hesabu; kwa maana Wasido-
ni[m] na Watiro[n] walimletea Dau-
di mbao za mierezi kwa wingi
sana. **5** Kwa hiyo Daudi aka-
sema: "Sulemani mwanangu ni
mchanga na mwororo,[o] na ile
nyumba itakayojengewa Yeho-
va inapaswa kuwa yenye utu-

SURA 21

a Law 9:24
1Fa 18:38
2Nya 7:1
b 2Sa 24:16
Zb 103:20
c 2Sa 24:25
d 1Fa 3:4
1Nya 16:39
2Nya 1:3
e 2Sa 6:9
Zb 119:120

SURA 22

f Kum 12:5
2Nya 3:1
g 2Sa 24:18
h 1Fa 9:21
2Nya 2:17
i 1Fa 5:17
j 1Fa 6:7
1Fa 7:9
k 1Fa 7:47
l 2Sa 5:11
m 1Fa 5:6
n 2Nya 2:3
o 1Fa 3:7
1Nya 29:1

Safu ya 2

a 2Nya 2:5
Zb 68:29
b Isa 64:11
Hag 2:3
c Mhu 9:10
d 2Sa 7:2
1Fa 8:17
Zb 132:5
e Kum 12:5
f 1Nya 28:3
g 1Fa 5:3
h 1Nya 17:4
2Nya 6:9
i 2Sa 7:12
1Nya 28:5
j 1Fa 4:25
1Fa 5:4
k 2Sa 12:24
l Zb 72:7
Isa 9:7
m 1Fa 5:5
1Nya 17:12
n 1Nya 17:13
o 2Sa 7:14
Ebr 1:5
p 1Nya 17:14
Zb 89:36
q 1Nya 28:20
r 2Nya 1:10
Zb 72:1
s Kum 4:6
Zb 19:11
t Yos 1:8
1Fa 2:3

kufu[a] zaidi kwa ajili ya uzuri[b]
wenye heshima kwa nchi zote.
Basi, acha mimi nimfanyie ma-
tayarisho." Hivyo Daudi akafa-
nya matayarisho kwa wingi
sana kabla ya kifo chake.[c]

6 Tena akamwita Sulemani
mwana wake ili ampe amri
ya kumjengea nyumba Yeho-
va, Mungu wa Israeli. **7** Naye
Daudi akamwambia Sulema-
ni mwana wake: "Kwa haba-
ri yangu, nilitaka sana moyoni[d]
mwangu kujenga nyumba kwa
ajili ya jina[e] la Yehova, Mu-
ngu wangu. **8** Lakini neno
la Yehova lilikuja dhidi yangu,
na kusema, 'Umemwaga damu
nyingi sana,[f] nawe umepiga-
na vita vikubwa.[g] Wewe hu-
tajenga nyumba kwa ajili ya
jina langu,[h] kwa kuwa ume-
mwaga damu nyingi sana du-
niani mbele zangu. **9** Tazama!
Utazaa mwana.[i] Yeye ataku-
wa mtu mtulivu, nami nita-
mpa pumziko kutoka kwa adui
zake wote pande zote;[j] kwa ma-
ana jina lake litakuwa Sule-
mani,[k] nami nitaleta juu ya
Israeli amani[l] na utulivu ka-
tika siku zake. **10** Yeye ndiye
atakayejenga nyumba kwa aji-
li ya jina langu,[m] naye ataku-
wa mwanangu,[n] nami nitakuwa
baba[o] yake. Nami hakika nita-
kifanya imara kiti cha ufalme[p]
wake juu ya Israeli mpaka wa-
kati usio na kipimo.'

11 "Sasa, mwanangu, Yeho-
va na awe pamoja nawe, nawe
upate mafanikio, ujenge nyu-
mba ya Yehova, Mungu wako,
kama alivyosema kukuhusu
wewe.[q] **12** Ila tu Yehova aku-
pe busara na uelewaji,[r] naye
akupe amri kuhusu Israeli ili
kuishika sheria ya Yehova, Mu-
ngu wako.[s] **13** Hivyo utapata
mafanikio[t] ukiangalia kutenda

masharti[a] na maamuzi ya hukumu[b] ambayo Yehova alimwamuru[c] Musa kuhusu Israeli. Uwe hodari na mwenye nguvu.[d] Usiogope[e] wala usiingiwe na hofu.[f] **14** Na tazama, wakati wa mateso[g] yangu nimetayarisha kwa ajili ya nyumba ya Yehova talanta mia moja elfu za dhahabu[h] na talanta milioni moja za fedha, na hakuna namna ya kupima uzito wa shaba[i] na chuma[j] kwa sababu zimekuwa nyingi sana; nami nimetayarisha mbao na mawe, lakini utaviongeza vitu hivyo. **15** Nawe una wafanyakazi wengi sana, wachongaji wa mawe na wafanyakazi wa mawe[k] na kila mwenye ustadi katika kila namna ya kazi.[l] **16** Hakuna namna yoyote ya kuhesabu dhahabu, fedha na shaba na chuma.[m] Simama, utende,[n] na Yehova awe pamoja nawe."[o]

17 Tena Daudi akawaamuru wakuu wote wa Israeli wamsaidie Sulemani mwana wake: **18** "Je, Yehova, Mungu wenu, hayuko pamoja nanyi,[p] na je, hakuwapa pumziko kuzunguka pande zote?[q] Kwa maana ametia mkononi mwangu wakaaji wa nchi, na nchi imetiishwa mbele za Yehova[r] na mbele ya watu wake. **19** Basi kazeni mioyo yenu na nafsi[s] zenu kumuuliza Yehova, Mungu wenu,[t] na msimame, mjenge patakatifu[u] pa Yehova, Mungu wa kweli,[v] ili kuleta sanduku[w] la agano la Yehova na vyombo vitakatifu vya Mungu wa kweli katika nyumba iliyojengwa kwa ajili ya jina[x] la Yehova."

23 Na Daudi alikuwa amezeeka[y] na kushiba siku, basi akamfanya Sulemani[z] mwana wake kuwa mfalme juu ya Israeli. **2** Ndipo akawakusanya wakuu[a] wote wa Israeli na makuhani[b] na Walawi.[c] **3** Basi Walawi wakahesabiwa kuanzia umri wa miaka 30 na zaidi;[d] na hesabu yao, kichwa kwa kichwa, mwanamume kwa mwanamume, ikawa 38,000. **4** Kati ya hao kwa ajili ya kuwa wasimamizi juu ya kazi ya nyumba ya Yehova kulikuwa na 24,000; na 6,000 kuwa maofisa[e] na waamuzi;[f] **5** na watunza-malango[g] 4,000 na watu 4,000 wenye kutoa sifa[h] kwa Yehova kwa vyombo[i] ambavyo Daudi alisema "Nimevitengeneza kwa ajili ya kutoa sifa."

6 Kisha Daudi akawagawa katika migawanyo[j] kwa wana wa Lawi,[k] kwa Gershoni, Kohathi na Merari. **7** Kwa Wagershoni, Ladani na Shimei. **8** Wana wa Ladani walikuwa Yehieli[l] akiwa kichwa na Zethamu na Yoeli,[m] watatu. **9** Wana wa Shimei walikuwa Shelomothi na Hazieli na Harani, watatu. Hao ndio waliokuwa vichwa vya upande wa baba kwa ajili ya Ladani. **10** Na wana wa Shimei walikuwa Yahathi, Zina na Yeushi na Beria. Hao wanne ndio waliokuwa wana wa Shimei. **11** Naye Yahathi akawa kichwa, Ziza wa pili. Nao Yeushi na Beria hawakuwa na wana wengi; kwa hiyo wakawa nyumba moja ya ukoo wa upande wa baba[n] kwa ajili ya tabaka moja rasmi.

12 Wana wa Kohathi[o] walikuwa Amramu, Ishari,[p] Hebroni[q] na Uzieli,[r] wanne. **13** Wana wa Amramu walikuwa Haruni[s] na Musa.[t] Lakini Haruni akatengwa[u] ili atakase Patakatifu Zaidi,[v] yeye na wanawe mpaka wakati usio na kipimo, kufukiza moshi wa dhabihu[w] mbele za Yehova, kumhudumia[x] na kutangaza baraka[y] katika jina lake mpaka wakati usio na kipimo.

SURA 22
a Kum 12:1
Kum 17:19
b Law 19:37
1Nya 28:7
c Hes 36:13
d Yos 1:6
1Nya 28:20
e Kum 31:6
f Yos 1:9
2Ti 1:7
g Ayu 14:1
Ro 8:22
h 1Nya 29:4
i 1Nya 29:2
j 1Nya 29:7
k 1Fa 5:17
1Fa 6:7
1Fa 7:9
l 1Fa 7:14
Met 22:29
m 1Nya 22:3
n Flp 2:13
o 2Nya 1:1
Ro 8:31
p Amu 6:12
q 2Sa 7:1
Met 16:7
r 2Sa 5:20
Zb 44:2
s Kum 4:29
t 2Nya 20:3
Da 9:3
u 2Nya 20:8
v 1Fa 6:1
w 1Fa 8:6
1Fa 8:21
2Nya 5:7
x Kum 12:21
1Fa 8:29
1Fa 9:3

SURA 23
y 1Fa 1:1
z 1Fa 1:33
1Fa 1:39
1Nya 28:5

Safu ya 2
a 1Nya 22:17
1Nya 28:1
b Kut 29:9
c Hes 3:6
1Nya 13:2
d Hes 4:3
e 1Nya 26:29
f Kum 16:18
2Nya 19:8
g 1Nya 26:12
h 1Nya 6:31
1Nya 9:33
i 1Fa 10:12
j 2Nya 8:14
2Nya 31:2
k Kut 6:16
l 1Nya 26:21
m 1Nya 26:22
n 1Nya 24:4
o Kut 6:18
p Kut 6:21
q Hes 3:27
r 1Nya 6:2
s Kut 4:14
t Kut 6:20
Kut 6:26
u Kut 28:1
Ebr 5:4
v Ebr 9:7
w 1Sa 2:28
x Kum 21:5
y Law 9:22
Hes 6:23

14 Naye Musa yule mtu wa Mungu wa kweli,[a] wanawe waliendelea kuhesabiwa kati ya kabila la Walawi.[b] **15** Wana wa Musa walikuwa Gershomu[c] na Eliezeri.[d] **16** Wana wa Gershomu walikuwa Shebueli[e] akiwa kichwa. **17** Na wana wa Eliezeri wakawa ni Rehabia[f] akiwa kichwa; na Eliezeri hakupata kuwa na wana wengine, lakini wana wa Rehabia wakawa wengi mno. **18** Wana wa Ishari[g] walikuwa Shelomithi[h] akiwa ndiye mwanamume aliye kichwa. **19** Wana wa Hebroni walikuwa Yeria akiwa kichwa, Amaria wa pili, Yahazieli wa tatu na Yekameamu[i] wa nne. **20** Wana wa Uzieli[j] walikuwa Mika akiwa kichwa na Ishia wa pili.

21 Wana wa Merari[k] walikuwa Mali na Mushi.[l] Wana wa Mali walikuwa Eleazari[m] na Kishi. **22** Lakini Eleazari akafa; naye hakuwa amepata wana, isipokuwa mabinti. Basi wana wa Kishi ndugu zao wakawachukua wawe wake zao.[n] **23** Wana wa Mushi walikuwa Mali na Ederi na Yeremothi,[o] watatu.

24 Hawa ndio waliokuwa wana wa Lawi kulingana na nyumba za baba zao,[p] vichwa vya upande wa akina baba, kulingana na watu wao waliopewa utume, katika hesabu ya majina, kwa vichwa vyao, wafanyakazi kwa ajili ya utumishi[q] wa nyumba ya Yehova, kuanzia umri wa miaka 20 na zaidi.[r] **25** Kwa maana Daudi alikuwa amesema: "Yehova, Mungu wa Israeli, amewapa watu wake pumziko,[s] naye atakaa Yerusalemu mpaka wakati usio na kipimo.[t] **26** Na pia Walawi hawataibeba tena maskani au chochote kati ya vyombo vyake kwa ajili ya utumishi wake."[a] **27** Kwa maana kwa maneno[b] ya mwisho ya Daudi hao ndio waliokuwa hesabu ya wana wa Lawi kuanzia umri wa miaka 20 na zaidi. **28** Kwa maana utendaji wao ulikuwa chini ya mwelekezo wa wana wa Haruni[c] kwa ajili ya utumishi wa nyumba ya Yehova juu ya nyua[d] na juu ya vyumba vya kulia chakula[e] na juu ya utakaso wa kila kitu kitakatifu[f] na kazi ya utumishi wa nyumba ya Mungu wa kweli, **29** kwa ajili ya mkate wa tabaka[g] na kwa ajili ya unga laini[h] wa toleo la nafaka na kwa ajili ya mkate mwembamba[i] usio na chachu[j] na kwa ajili ya keki za kuoka[k] na kwa ajili ya unga wa kukandwa uliochanganywa[l] na kwa ajili ya vipimo vyote vya wingi na ukubwa;[m] **30** na kwa ajili ya kusimama[n] kila asubuhi[o] ili kumshukuru[p] na kumsifu[q] Yehova, na wakati wa jioni vivyo hivyo; **31** na kwa ajili ya kila toleo la dhabihu za kuteketezwa kwa Yehova katika sabato,[r] katika miezi mipya[s] na katika majira ya sherehe,[t] kufuatilia hesabu kulingana na kanuni zenye kuzihusu, daima mbele za Yehova. **32** Nao wakafanya ulinzi wa hema la mkutano na ulinzi[u] wa mahali patakatifu[v] na ulinzi wa wana wa Haruni ndugu zao kwa ajili ya utumishi wa nyumba ya Yehova.[w]

24 Basi wana wa Haruni walikuwa na migawanyo yao. Wana wa Haruni walikuwa Nadabu[x] na Abihu,[y] Eleazari[z] na Ithamari.[a] **2** Hata hivyo, Nadabu na Abihu[b] walikufa kabla ya baba yao,[c] nao hawakuwa na wana wowote, bali Eleazari[d] na Ithamari wakaendelea kuwa makuhani. **3** Na Daudi,

SURA 23

a Zb 90:Uta
b 1Nya 26:24
c Kut 2:22
d Kut 18:4
e 1Nya 26:24
f 1Nya 26:25
g Hes 3:27
h 1Nya 24:22
i 1Nya 24:23
j Kut 6:22
k Kut 6:19
l Hes 26:58
1Nya 24:30
m 1Nya 24:28
n Hes 36:11
o 1Nya 24:30
p Hes 26:58
q 1Nya 28:13
r Ezr 3:8
s 2Sa 7:1
1Nya 22:18
t 1Fa 8:13
Zb 135:21

Safu ya 2

a Hes 4:15
Hes 4:49
b 2Sa 23:2
c Hes 3:9
d 1Fa 6:36
e 1Nya 9:26
f Ne 12:45
g Law 24:6
1Nya 9:32
h 1Nya 9:29
i Kut 29:23
Law 2:4
j Kut 29:2
k Law 7:9
l Law 7:12
m Law 19:36
n 1Nya 16:37
o Kut 29:39
p Law 22:29
Zb 105:1
Flp 4:6
q 1Nya 16:4
Zb 69:30
2Ko 11:31
r Kut 20:10
s Hes 10:10
Zb 81:3
t Law 23:4
u Hes 1:53
v 1Nya 9:27
w Hes 3:9

SURA 24

x Kut 6:23
y Law 10:1
z Kut 28:1
a Hes 3:2
b Kut 6:23
c Hes 26:61
d Hes 16:39

na Sadoki[a] kutoka kwa wana wa Eleazari, na Ahimeleki[b] kutoka kwa wana wa Ithamari wakawafanya wawe migawanyo kwa ajili ya cheo chao katika utumishi wao.[c] **4** Lakini wana wa Eleazari wakaonekana kuwa na wanaume wengi waliokuwa vichwa kuliko wana wa Ithamari. Basi wakawagawa kwa wana wa Eleazari, wawe vichwa vya nyumba za ukoo wao wa upande wa baba, kumi na sita, na kwa wana wa Ithamari, wawe vichwa vya nyumba zao za ukoo wa upande wa baba, wanane.

5 Tena, wakawagawa kwa kura,[d] hawa pamoja na wale, kwa maana kulipaswa kuwa na wakuu wa mahali patakatifu[e] na wakuu wa Mungu wa kweli kutoka kwa wana wa Eleazari na kutoka kwa wana wa Ithamari. **6** Ndipo Shemaya mwana wa Nethaneli mwandishi[f] wa Walawi akawaandika mbele ya mfalme na wakuu na Sadoki[g] kuhani na Ahimeleki[h] mwana wa Abiathari[i] na vichwa vya baba za makuhani na vya Walawi,[j] nyumba moja ya ukoo wa upande wa baba ikichaguliwa kwa ajili ya Eleazari[k] na moja ikichaguliwa kwa ajili ya Ithamari.[l]

7 Na kura ikatoka: ya kwanza ya Yehoyaribu;[m] ya pili ya Yedaya, **8** ya 3 ya Harimu, ya 4 ya Seorimu, **9** ya 5 ya Malkiya, ya 6 ya Miyamini, **10** ya 7 ya Hakozi, ya 8 ya Abiya,[n] **11** ya 9 ya Yeshua, ya 10 ya Shekania, **12** ya 11 ya Eliashibu, ya 12 ya Yakimu, **13** ya 13 ya Hupa, ya 14 ya Yeshebeabu, **14** ya 15 ya Bilga, ya 16 ya Imeri, **15** ya 17 ya Heziri, ya 18 ya Hapisesi, **16** ya 19 ya Pethahia, ya 20 ya Yehezkeli, **17** ya 21 ya Yakini, ya 22 ya Gamuli, **18** ya 23 ya Delaya, ya 24 ya Maazia.

19 Hivi ndivyo vilivyokuwa vyeo[a] vyao kwa ajili ya utumishi wao,[b] kuingia katika nyumba ya Yehova kulingana na haki yao[c] inayostahiliwa kwa mkono wa Haruni babu yao, kama vile Yehova, Mungu wa Israeli, alivyokuwa amemwamuru.

20 Na wa wana wa Lawi waliobaki, wa wana wa Amramu[d] kulikuwa na Shubaeli;[e] wa wana wa Shubaeli, Yehdeya; **21** wa Rehabia:[f] wa wana wa Rehabia, Ishia akiwa kichwa; **22** wa Waishari,[g] Shelomothi;[h] wa wana wa Shelomothi, Yahathi; **23** na wana wa Hebroni,[i] Yeria[j] akiwa kichwa, Amaria wa pili, Yahazieli wa tatu, Yekameamu wa nne. **24** Wana wa Uzieli, Mika; wa wana wa Mika,[k] Shamiri. **25** Ndugu ya Mika alikuwa Ishia; wa wana wa Ishia, Zekaria.

26 Wana wa Merari[l] walikuwa Mali[m] na Mushi;[n] wana wa Yaazia, Beno. **27** Wana wa Merari: Wa Yaazia, Beno na Shohamu na Zakuri na Ibri. **28** Wa Mali, Eleazari, ambaye hakupata wana wowote.[o] **29** Wa Kishi: wana wa Kishi walikuwa Yerahmeeli. **30** Na wana wa Mushi walikuwa Mali[p] na Ederi na Yerimothi.[q]

Hao ndio waliokuwa wana wa Walawi kulingana na nyumba za ukoo wa upande wa baba[r] zao. **31** Nao wenyewe pia wakapiga kura[s] sawasawa na walivyofanya ndugu zao wana wa Haruni mbele ya Daudi mfalme, na Sadoki na Ahimeleki na vichwa vya nyumba za ukoo wa upande wa baba vya makuhani na vya Walawi. Na kwa habari ya nyumba za

SURA 24

a 1Nya 6:8
b 2Sa 8:17
c 1Ko 14:33
d Met 16:33
Met 18:18
Mdo 1:26
e Mt 26:3
f 1Fa 4:3
2Nya 34:13
g 1Fa 2:35
h 2Sa 8:17
i 2Sa 19:11
1Fa 1:7
j 1Nya 23:24
k Law 10:12
Hes 16:39
l 1Nya 6:3
m Ne 11:10
n Lu 1:5

Safu ya 2

a 1Nya 9:25
2Nya 23:18
b Lu 1:8
Lu 1:23
c 2Fa 11:9
1Ko 14:40
d Kut 6:18
e 1Nya 23:16
1Nya 26:24
f 1Nya 23:17
g Hes 3:27
h 1Nya 23:18
i Hes 26:58
1Nya 15:9
j 1Nya 23:19
1Nya 26:31
k 1Nya 23:20
l Mwa 46:11
Kut 6:19
m 1Nya 6:19
n 1Nya 23:21
o 1Nya 23:22
p 1Nya 6:47
q 1Nya 23:23
r 1Nya 23:11
s Yos 18:10
1Nya 25:8
Met 16:33
Mdo 1:26

ukoo wa upande wa baba,[a] aliye
kichwa alikuwa sawasawa na
ndugu yake mdogo.

25 Tena Daudi na wakuu[b] wa
vikundi vya utumishi[c] wa-
katenga kwa ajili ya utumishi
sehemu ya wana wa Asafu, He-
mani[d] na Yeduthuni[e] wenye kuto-
a unabii kwa vinubi,[f] kwa vina-
nda[g] na kwa matoazi.[h] Na kuto-
ka katika hesabu yao kukawa na
wanaume rasmi kwa ajili ya utu-
mishi wao. **2** Wa wana wa Asa-
fu, Zakuri na Yosefu[i] na Netha-
nia na Asharela,[j] wana wa Asafu
chini ya amri ya Asafu[k] mwenye
kutoa unabii chini ya mfalme.
3 Wa Yeduthuni:[l] wana wa Ye-
duthuni, Gedalia[m] na Zeri[n] na
Yeshaya,[o] na Shimei, Hashabia
na Matithia,[p] sita, chini ya amri
ya Yeduthuni baba yao, aliyeku-
wa akitoa unabii akiwa na ki-
nubi kwa ajili ya kumshukuru
na kumsifu Yehova.[q] **4** Wa He-
mani:[r] wana wa Hemani, Bu-
kia,[s] Matania,[t] Uzieli,[u] Shebueli
na Yerimothi, Hanania,[v] Hanani,
Eliatha,[w] Gidalti[x] na Romamti-
ezeri,[y] Yoshbekasha,[z] Malothi,[a]
Hothiri,[b] Mahaziothi. **5** Hawa
wote ndio waliokuwa wana wa
Hemani, mwonaji[c] wa mfalme
katika mambo ya Mungu wa
kweli ili ainue pembe yake; basi
Mungu wa kweli akampa Hema-
ni wana kumi na wanne na bi-
nti watatu.[d] **6** Hawa wote ndio
waliokuwa chini ya amri ya baba
yao katika nyimbo kwenye nyu-
mba ya Yehova, wakiwa na mato-
azi,[e] vinanda[f] na vinubi[g] kwa aji-
li ya utumishi wa nyumba ya Mu-
ngu wa kweli.

Chini ya amri ya mfalme ku-
likuwa Asafu na Yeduthuni na
Hemani.[h]

7 Na hesabu yao pamoja na
ndugu zao waliozoezwa nyi-
mbo kwa Yehova,[a] wote waki-
wa wajuzi,[b] ikawa 288. **8** Basi
wakapiga kura[c] kuhusu vitu vi-
navyopaswa kutunzwa, mdogo
akiwa sawasawa na mkubwa,[d]
mwenye ujuzi[e] pamoja na mwe-
nye kujifunza.

9 Na kura ikatoka: ya kwa-
nza ya Asafu kwa ajili ya Yo-
sefu,[f] ya pili ya Gedalia[g] (yeye
na ndugu zake na wanawe wali-
kuwa 12); **10** ya tatu ya Zaku-
ri,[h] wanawe na ndugu zake, 12;
11 ya 4 ya Izri,[i] wanawe na ndu-
gu zake, 12; **12** ya 5 ya Netha-
nia,[j] wanawe na ndugu zake, 12;
13 ya 6 ya Bukia, wanawe na
ndugu zake, 12; **14** ya 7 ya
Yesharela,[k] wanawe na ndugu
zake, 12; **15** ya 8 ya Yesha-
ya, wanawe na ndugu zake, 12;
16 ya 9 ya Matania, wanawe
na ndugu zake, 12; **17** ya 10
ya Shimei, wanawe na ndugu
zake, 12; **18** ya 11 ya Azare-
li,[l] wanawe na ndugu zake, 12;
19 ya 12 ya Hashabia, wanawe
na ndugu zake, 12; **20** ya 13,
ya Shubaeli,[m] wanawe na ndu-
gu zake, 12; **21** ya 14, ya Ma-
tithia, wanawe na ndugu
zake, 12; **22** ya 15, ya Yeremo-
thi, wanawe na ndugu zake, 12;
23 ya 16, ya Hanania, wanawe
na ndugu zake, 12; **24** ya 17, ya
Yoshbekasha, wanawe na ndu-
gu zake, 12; **25** ya 18, ya Ha-
nani, wanawe na ndugu zake, 12;
26 ya 19, ya Malothi, wanawe na
ndugu zake, 12; **27** ya 20, ya
Eliatha, wanawe na ndugu
zake, 12; **28** ya 21, ya Hothi-
ri, wanawe na ndugu zake, 12;
29 ya 22, ya Gidalti, wanawe na
ndugu zake, 12; **30** ya 23, ya
Mahaziothi,[n] wanawe na ndu-
gu zake, 12; **31** ya 24, ya Ro-
mamti-ezeri,[o] wanawe na ndugu
zake, 12.

SURA 24
a 1Nya 26:13

SURA 25
b 1Nya 24:5
c 1Nya 27:3
d 1Nya 16:41
2Nya 5:12
e 2Nya 35:15
f 1Fa 10:12
Zb 81:2
g 1Sa 10:5
1Nya 15:16
h 2Nya 29:25
Zb 150:5
i 1Nya 25:9
j 1Nya 25:14
k Ne 12:46
l 1Nya 16:42
m 1Nya 25:9
n 1Nya 25:11
o 1Nya 25:15
p 1Nya 15:18
q Zb 92:1
Yer 33:11
Efe 5:19
r 1Nya 15:19
s 1Nya 25:13
t 1Nya 25:16
u 1Nya 24:24
v 1Nya 25:23
w 1Nya 25:27
x 1Nya 25:29
y 1Nya 25:31
z 1Nya 25:24
a 1Nya 25:26
b 1Nya 25:28
c 1Sa 9:9
d Zb 127:3
Isa 8:18
e 1Nya 13:8
f 1Nya 15:16
g 1Nya 16:5
h 1Nya 25:1

Safu ya 2
a Zb 150:1
b 1Nya 15:22
c Met 16:33
Met 18:18
Mdo 1:26
d 1Nya 24:31
e 1Nya 15:22
f 1Nya 25:2
g 1Nya 25:3
h 1Nya 25:2
i 1Nya 25:3
j 1Nya 25:2
k 1Nya 25:2
l 1Nya 25:4
m 1Nya 25:4
n 1Nya 25:4
o 1Nya 25:4

26 Kwa ajili ya migawanyo
ya watunza-malango:[a] Wa
Wakora,[b] Meshelemia[c] mwa-
na wa Kore wa wana wa Asa-
fu. **2** Na Meshelemia aliku-
wa na wana: Zekaria mzaliwa
wa kwanza, Yediaeli wa pili, Ze-
badia wa tatu, Yathnieli wa nne,
3 Elamu wa tano, Yehohanani
wa sita, Elieho-enai wa saba.
4 Na Obed-edomu[d] alikuwa na
wana: Shemaya mzaliwa wa
kwanza, Yehozabadi wa pili,
Yoa wa tatu na Sakari wa nne
na Nethaneli wa tano, **5** Ami-
eli wa sita, Isakari wa saba, Peu-
lethai wa nane; kwa maana Mu-
ngu alikuwa amembariki.[e]
6 Naye Shemaya mwana
wake alizaa wana waliokuwa
watawala wa nyumba ya baba
yao, kwa kuwa walikuwa wanau-
me wenye uwezo, wenye nguvu.
7 Wana wa Shemaya, Othni
na Refaeli na Obedi, Elzaba-
di, ambaye ndugu zake waliku-
wa wanaume wenye uwezo, Eli-
hu na Semakia. **8** Hawa wote
ndio waliokuwa wa wana wa
Obed-edomu, wao na wana wao
na ndugu zao, wanaume wenye
uwezo na wenye mamlaka kwa
ajili ya utumishi, 62 wa Obed-
edomu. **9** Na Meshelemia[f] ali-
kuwa na wana na ndugu, wa-
naume wenye uwezo, kumi na
wanane. **10** Na Hosa wa wana
wa Merari alikuwa na wana.
Shimri ndiye aliyekuwa ki-
chwa, kwa maana hakuwa mza-
liwa wa kwanza[g] lakini baba
yake akamweka kuwa kichwa;[h]
11 Hilkia wa pili, Tebalia wa
tatu, Zekaria wa nne. Wana
wote na ndugu za Hosa waliku-
wa kumi na watatu.
12 Kati ya hii migawanyo
ya watunza-malango, wana-
ume walio vichwa walikuwa na
kazi sawasawa na ndugu zao
walivyokuwa nayo,[a] kuhudu-
mu katika nyumba ya Yeho-
va. **13** Basi wakapiga kura[b]
kwa ajili ya mdogo sawasawa
na kwa mkubwa kulingana na
nyumba za ukoo wa upande
wa baba[c] zao, kwa ajili ya
malango mbalimbali. **14** Ndi-
po kura ya upande wa mashari-
ki ikamwangukia Shelemia.[d]
Kwa ajili ya Zekaria[e] mwana
wake, mshauri[f] mwenye busa-
ra, walipiga kura, na kura
yake ikawa upande wa kaskazi-
ni.[g] **15** Obed-edomu akawa na
yake upande wa kusini, na wa-
nawe[h] wakawa na maghala.[i]
16 Shupimu na Hosa[j] wakawa
na yao upande wa magharibi
karibu na Lango la Shale-
kethi kando ya njia kuu ina-
yopanda kwenda juu, kikundi
cha ulinzi[k] kikilingana na kiku-
ndi cha ulinzi;[l] **17** upande wa
mashariki kulikuwa na Walawi
sita; upande wa kaskazini kila
siku, wanne; upande wa kusi-
ni kila siku,[m] wanne; na kwa
ajili ya maghala,[n] wawili wawi-
li; **18** kwa ajili ya roshani upa-
nde wa magharibi, wanne ka-
ndo ya njia kuu,[o] wawili kwenye
roshani. **19** Hiyo ilikuwa mi-
gawanyo ya watunza-malango
ya wana wa Wakora[p] na ya wana
wa Merari.[q]
20 Kwa habari ya Walawi,
Ahiya alikuwa juu ya hazina[r]
za nyumba ya Mungu wa kwe-
li na juu ya hazina za vitu vi-
livyofanywa kuwa vitakatifu.[s]
21 Wana wa Ladani,[t] wana wa
Mgershoni wa Ladani; walio vi-
chwa vya nyumba za ukoo wa
upande wa baba wa Ladani
Mgershoni, Yehieli.[u] **22** Wana
wa Yehieli, Zethamu na Yoe-
li[v] ndugu yake, walikuwa juu
ya hazina[w] za nyumba ya Yeho-
va. **23** Kwa ajili ya Waamra-

SURA 26
a 1Nya 9:22
2Nya 23:19
b Hes 26:11
Zb 44:Uta
Zb 49:Uta
c 1Nya 26:14
d 1Nya 16:38
e Kum 28:11
Zb 127:3
f 1Nya 26:14
g Kum 21:17
h 1Nya 5:1

Safu ya 2
a 1Nya 25:8
b Met 16:33
Met 18:18
Mdo 1:26
c 1Nya 23:11
d 1Nya 26:1
e 1Nya 26:2
f 1Nya 27:32
Met 12:8
1Ti 3:13
g 1Nya 9:24
h 1Nya 26:4
i 2Nya 25:24
j 1Nya 26:10
k 1Nya 23:32
l Ne 12:24
m 2Nya 8:14
n 1Nya 26:15
o 1Nya 26:16
p Hes 26:11
Zb 44:Uta
Zb 49:Uta
q 1Nya 23:6
r 1Fa 14:26
1Nya 9:26
s 1Fa 7:51
1Nya 18:11
t 1Nya 23:7
u 1Nya 29:8
v 1Nya 23:8
w 1Fa 15:18

mu, kwa ajili ya Waishari, kwa
ajili ya Wahebroni, kwa ajili
ya Wauzieli,[a] **24** hata Shebue-
li[b] mwana wa Gershomu mwa-
na wa Musa alikuwa kiongozi
juu ya maghala. **25** Kwa ha-
bari ya ndugu zake, wa Eliezeri[c]
kulikuwa na Rehabia[d] mwana
wake na Yeshaya mwana wake
na Yoramu mwana wake na Zi-
kri mwana wake na Shelomothi
mwana wake. **26** Huyu Shelo-
mothi na ndugu zake walikuwa
juu ya hazina zote za vitu vili-
vyofanywa kuwa vitakatifu,[e]
ambavyo Daudi[f] mfalme na wa-
lio vichwa vya nyumba za ukoo
wa upande wa baba,[g] na wa-
kuu wa maelfu na wa mamia,
na wakuu wa jeshi walikuwa
wamevifanya kuwa vitakatifu.
27 Walikuwa wamefanya vitu
kuwa vitakatifu kutoka katika
vita[h] na kutoka katika nyara[i]
ili kuidumisha nyumba ya Ye-
hova. **28** Na pia vyote amba-
vyo Samweli mwonaji[j] na Sau-
li mwana wa Kishi na Abneri[k]
mwana wa Neri na Yoabu[l] mwa-
na wa Seruya[m] walikuwa wame-
vifanya kuwa vitakatifu. Cho-
chote ambacho mtu alikifanya
kuwa kitakatifu kilikuwa chini
ya Shelomithi na ndugu zake.

29 Wa Waishari,[n] Kenania
na wanawe walikuwa kwa ajili
ya shughuli za nje[o] wakiwa ma-
ofisa na waamuzi[p] juu ya Israeli.

30 Wa Wahebroni,[q] Hashabia
na ndugu zake, wanaume we-
nye uwezo,[r] elfu moja na mia
saba, walikuwa juu ya usima-
mizi wa Israeli katika eneo
la Yordani upande wa maghari-
bi kwa ajili ya kazi yote ya Ye-
hova na kwa ajili ya utumishi
wa mfalme. **31** Wa Wahebro-
ni, Yeriya[s] alikuwa kichwa cha
Wahebroni kulingana na viza-
zi vyao kulingana na mababu

SURA 26

a Hes 3:27
b 1Nya 24:20
c Kut 18:4
d 1Nya 23:17
e Hes 31:50
1Nya 18:11
f 1Nya 29:3
g 1Nya 29:7
h Yos 6:19
i Hes 31:28
j 1Sa 9:9
k 1Sa 14:50
l 2Sa 20:23
m 2Sa 2:18
n 1Nya 23:12
o Ne 11:16
p Kum 17:9
2Nya 19:8
q 1Nya 23:12
1Nya 23:19
r 1Nya 26:6
s 1Nya 23:19

Safu ya 2

a 2Sa 5:4
1Nya 29:27
b Yos 13:25
Yos 21:39
c Mwa 31:21
1Sa 13:7
d 1Nya 26:9
e 1Nya 24:31
f 1Nya 12:37
g 2Nya 19:11

SURA 27

h 1Nya 5:24
i Kut 18:25
1Sa 8:12
1Nya 13:1
2Nya 1:2
j Kum 1:15
k 1Nya 28:1
l 2Sa 23:8
1Nya 11:11
m Hes 26:21
n 2Sa 23:9
1Nya 11:12
o 1Nya 8:4
p 2Sa 23:20
q 1Fa 4:4
1Nya 12:27

zao. Walitafutwa katika mwa-
ka wa 40[a] wa ufalme wa Dau-
di, nao mashujaa, wanaume we-
nye nguvu wakapatikana kati
yao huko Yazeri[b] katika Gilea-
di.[c] **32** Na ndugu zake, wa-
naume wenye uwezo,[d] walikuwa
elfu mbili na mia saba, wa-
lio vichwa vya nyumba za ukoo
wa upande wa baba.[e] Basi Dau-
di mfalme akawapa mgawo
kuwa juu ya Warubeni na Wa-
gadi na nusu ya kabila la Wa-
manase,[f] kwa ajili ya kila jambo
la Mungu wa kweli na jambo[g] la
mfalme.

27 Kwa habari ya wana wa
Israeli kulingana na he-
sabu yao, walio vichwa vya nyu-
mba za ukoo wa upande wa
baba[h] na wakuu[i] wa maelfu
na wa mamia[j] na maofisa wao
waliomhudumia[k] mfalme kati-
ka kila jambo la ile migawa-
nyo ya wale walioingia na kuto-
ka mwezi kwa mwezi kwa mie-
zi yote ya mwaka, katika kila
mgawanyo kulikuwa na watu
24,000.

2 Juu ya mgawanyo wa kwa-
nza wa mwezi wa kwanza ku-
likuwa na Yashobeamu[l] mwa-
na wa Zabdieli, na katika mga-
wanyo wake kulikuwa na watu
24,000. **3** Baadhi ya wana wa
Perezi[m] aliye kichwa cha wa-
kuu wote wa vikundi vya utumi-
shi walikuwa kwa ajili ya mwezi
wa kwanza. **4** Na juu ya mga-
wanyo wa mwezi wa pili kuli-
kuwa na Dodai[n] Mwahohi[o] na
mgawanyo wake, na Miklothi
ndiye aliyekuwa kiongozi, na
katika mgawanyo wake kuliku-
wa na watu 24,000. **5** Mkuu
wa kikundi cha tatu cha utu-
mishi kwa ajili ya mwezi wa
tatu alikuwa ni Benaya[p] mwa-
na wa Yehoyada[q] mkuu wa ma-
kuhani, na katika mgawanyo

wake kulikuwa na watu 24,000.
6 Huyo Benaya[a] alikuwa mwanamume mwenye nguvu wa
wale 30[b] na juu ya wale 30;
na juu ya mgawanyo wake ku-
likuwa na Amizabadi mwana
wake. **7** Wa nne kwa ajili ya
mwezi wa nne alikuwa Asahe-
li,[c] ndugu ya Yoabu,[d] na Zeba-
dia mwana wake baada yake,
na katika mgawanyo wake wali-
kuwa 24,000. **8** Mkuu wa tano
kwa ajili ya mwezi wa tano aliku-
wa Shamhuthi[e] Mwizrahia, na
katika mgawanyo wake waliku-
wa 24,000. **9** Wa sita kwa aji-
li ya mwezi wa sita alikuwa Ira[f]
mwana wa Ikeshi[g] Mtekoa,[h] na
katika mgawanyo wake waliku-
wa 24,000. **10** Wa saba kwa aji-
li ya mwezi wa saba alikuwa He-
lezi[i] Mpeloni,[j] wa wana wa Efra-
imu, na katika mgawanyo wake
walikuwa 24,000. **11** Wa nane
kwa ajili ya mwezi wa nane ali-
kuwa Sibekai[k] Mhusha wa Wa-
zera,[l] na katika mgawanyo wake
walikuwa 24,000. **12** Wa tisa
kwa ajili ya mwezi wa tisa aliku-
wa Abiezeri[m] Mwanathothi[n] wa
Wabenyamini, na katika mga-
wanyo wake walikuwa 24,000.
13 Wa kumi kwa ajili ya mwezi
wa kumi alikuwa Maharai[o] Mne-
tofa wa Wazera,[p] na katika mga-
wanyo wake walikuwa 24,000.
14 Wa kumi na moja kwa ajili ya
mwezi wa kumi na moja alikuwa
Benaya[q] Mpirathoni wa wana wa
Efraimu,[r] na katika mgawanyo
wake walikuwa 24,000. **15** Wa
kumi na mbili kwa ajili ya mwe-
zi wa kumi na mbili alikuwa He-
ldai[s] Mnetofa, wa Othnieli, na
katika mgawanyo wake waliku-
wa 24,000.

16 Na juu ya makabila ya
Israeli,[t] wa Warubeni, Eliezeri mwana wa Zikri ndiye aliyekuwa kiongozi; wa Wasimeoni, Shefatia mwana wa Maaka;
17 wa Lawi, Hashabia mwana wa Kemueli; wa Haruni, Sadoki;[a] **18** wa Yuda, Elihu,[b] mmoja wa ndugu za Daudi;[c] wa Isakari, Omri mwana wa Mikaeli; **19** wa Zabuloni, Ishmaya mwana wa Obadia; wa Naftali, Yerimothi mwana wa Azrieli; **20** wa wana wa Efraimu, Hoshea mwana wa Azazia; wa nusu ya kabila la Manase, Yoeli mwana wa Pedaya; **21** wa nusu ya kabila la Manase katika Gileadi, Ido mwana wa Zekaria; wa Benyamini, Yaasieli mwana wa Abneri;[d] **22** wa Dani, Azareli mwana wa Yerohamu. Hao walikuwa wakuu[e] wa makabila ya Israeli.

23 Na Daudi hakuhesabu wale waliokuwa na umri wa miaka 20 kurudi chini, kwa sababu Yehova alikuwa ameahidi kufanya Israeli kuwa wengi kama nyota za mbinguni.[f]
24 Yoabu[g] mwana wa Seruya alikuwa ameanza kuhesabu, lakini hakumaliza;[h] na kwa sababu hiyo kukawa na ghadhabu[i] juu ya Israeli, na hesabu hiyo haikuwekwa katika hesabu ya mambo ya siku za Mfalme Daudi.

25 Na juu ya hazina za mfalme[j] kulikuwa na Azmavethi mwana wa Adieli. Na juu ya hazina katika shamba,[k] katika majiji[l] na katika vijiji na katika minara kulikuwa na Yonathani mwana wa Uzia. **26** Na juu ya wafanyakazi shambani,[m] kwa ajili ya kulima udongo, kulikuwa na Ezri mwana wa Kelubu. **27** Na juu ya mashamba ya mizabibu[n] kulikuwa na Shimei Mrama; na juu ya vitu vilivyokuwa katika mashamba ya mizabibu kwa ajili ya aki-

SURA 27
a 2Sa 23:20
b 2Sa 23:23
c 2Sa 2:18
2Sa 23:24
d 1Nya 2:16
e 2Sa 23:25
1Nya 11:27
f 2Sa 23:26
g 1Nya 11:28
h 2Nya 11:6
2Nya 20:20
Amo 1:1
i 1Nya 11:27
j 2Sa 23:26
k 2Sa 21:18
l Hes 26:20
m 2Sa 23:27
n 1Nya 6:60
o 2Sa 23:28
p Hes 26:20
q 2Sa 23:30
r Amu 12:15
s 2Sa 23:29
t Mdo 26:7

Safu ya 2
a 1Nya 24:31
b 1Sa 17:28
c 1Sa 16:6
d 1Sa 14:50
2Sa 3:27
e 1Nya 22:17
1Nya 28:1
f Mwa 15:5
Ebr 11:12
g 2Sa 24:2
h 1Nya 21:6
i 2Sa 24:15
1Nya 21:7
j 2Fa 18:15
k 1Sa 8:14
2Nya 26:10
l 1Fa 9:19
m Mhu 5:9
n 1Sa 8:14
1Sa 22:7

ba za divai kulikuwa na Zabdi Mshifi. **28** Na juu ya mashamba ya mizeituni na mikuyu[a] iliyokuwa katika Shefela[b] kulikuwa na Baal-hanani Mgederi; na juu ya akiba ya mafuta[c] kulikuwa na Yoashi. **29** Na juu ya mifugo iliyokuwa ikilisha katika Sharoni[d] kulikuwa na Shitrai Msharoni; na juu ya mifugo katika nchi tambarare za chini kulikuwa na Shafati mwana wa Adlai. **30** Na juu ya ngamia[e] kulikuwa na Obili Mwishmaeli;[f] na juu ya punda-jike kulikuwa na Yehdeya Mmeronothi. **31** Na juu ya makundi kulikuwa na Yazizi Mhagri. Hao wote ndio waliokuwa wakuu wa mali za Mfalme Daudi.

32 Na Yonathani,[g] mpwa wa Daudi, alikuwa mshauri, mwanamume mwenye uelewaji,[h] naye alikuwa mwandishi pia; na Yehieli mwana wa Hakmoni[i] alikuwa pamoja na wana wa mfalme.[j] **33** Na Ahithofeli[k] alikuwa mshauri[l] wa mfalme; na Hushai[m] Mwarki,[n] alikuwa rafiki ya mfalme.[o] **34** Na baada ya Ahithofeli kulikuwa na Yehoyada mwana wa Benaya[p] na Abiathari;[q] na Yoabu[r] alikuwa mkuu wa jeshi la mfalme.

28 Na Daudi akakusanya katika Yerusalemu wakuu[s] wote wa Israeli, wakuu[t] wa makabila na wakuu[u] wa migawanyo ya wale wanaomhudumia mfalme na wakuu wa maelfu[v] na wakuu wa mamia[w] na wakuu wa mali[x] zote na mifugo[y] ya mfalme na wa wanawe,[z] pamoja na maofisa wa makao[a] ya mfalme na wanaume wenye nguvu,[b] kila mwanamume shujaa, mwenye nguvu. **2** Kisha Daudi mfalme akasimama kwa miguu yake na kusema:

SURA 27

a 2Nya 9:27
b 2Nya 26:10
c 1Fa 5:11
2Nya 32:28
d Isa 35:2
e 1Sa 27:9
f Mwa 37:25
g 2Sa 13:3
2Sa 21:21
h Met 1:5
Met 10:13
Met 16:21
i 1Nya 11:11
j 2Sa 3:2
1Nya 3:5
k 2Sa 15:12
2Sa 16:23
2Sa 17:23
l Zb 119:24
m 2Sa 15:37
n 2Sa 16:16
o 2Sa 16:17
p 2Sa 23:20
1Fa 2:35
q 1Fa 1:7
r 1Nya 11:6

SURA 28

s Kum 31:28
Yos 23:2
t 1Nya 27:16
u 1Nya 27:1
v Kut 18:25
1Sa 8:12
w Kum 1:15
x 1Nya 27:25
y 1Nya 27:29
z 2Sa 3:2
1Nya 3:5
a 1Sa 8:15
b 1Nya 11:10

Safu ya 2

a 1Fa 8:17
Zb 132:5
b Zb 132:7
c 1Nya 22:3
d 2Sa 7:13
1Fa 5:3
1Nya 17:4
e 1Nya 22:8
f 1Sa 16:1
g 1Sa 16:13
2Sa 7:8
Zb 89:20
h Mwa 49:10
1Nya 5:2
Zb 60:7
i Ru 4:22
j 1Sa 16:11
k 1Sa 13:14
1Sa 16:12
l 2Sa 3:2
1Nya 3:5
m 1Nya 22:9
n 1Nya 17:14
2Nya 1:8
o 2Sa 7:13
p 1Nya 17:13
q 2Sa 7:14
r 1Nya 17:14
Zb 72:8
s 1Fa 6:12
t Kum 12:1
u 1Ti 3:15
v 1Ti 5:21
w Kum 6:3

"Nisikilizeni, ndugu zangu na watu wangu. Nilitaka sana moyoni mwangu[a] kujenga nyumba ya kupumzika kwa ajili ya sanduku la agano la Yehova na kama kiti cha miguu[b] cha Mungu wetu, nami nikawa nimefanya matayarisho ya kujenga.[c] **3** Naye Mungu wa kweli akaniambia, 'Hutajenga nyumba kwa ajili ya jina langu;[d] kwa maana wewe ni mtu wa vita, nawe umemwaga damu.'[e] **4** Basi Yehova, Mungu wa Israeli, alinichagua mimi kutoka katika nyumba yote ya baba yangu[f] niwe mfalme[g] juu ya Israeli mpaka wakati usio na kipimo; kwa maana alimchagua Yuda awe kiongozi,[h] na katika nyumba ya Yuda aliichagua nyumba ya baba yangu,[i] na kati ya wana wa baba yangu,[j] alinikubali mimi,[k] ili kunifanya niwe mfalme juu ya Israeli yote; **5** na kati ya wanangu wote (kwa maana wana ambao Yehova amenipa ni wengi)[l] ndipo akamchagua Sulemani[m] mwanangu aketi kwenye kiti cha ufalme[n] wa Yehova juu ya Israeli.

6 "Tena akaniambia, 'Sulemani mwana wako ndiye atakayejenga nyumba yangu[o] na nyua zangu; kwa maana nimemchagua yeye kuwa mwanangu,[p] nami nitakuwa baba yake.[q] **7** Nami kwa hakika nitaufanya imara ufalme wake[r] mpaka wakati usio na kipimo ikiwa ataazimia kwa nguvu kushika amri[s] zangu na maamuzi yangu ya hukumu,[t] kama ilivyo leo hii.' **8** Na sasa, mbele ya macho ya Israeli wote, kutaniko la Yehova,[u] na masikioni pa Mungu wetu,[v] iweni waangalifu na mtafute amri zote za Yehova, Mungu wenu, ili mpate kuimiliki nchi hii nzuri,[w]

na mpate kuipitisha kuwa urithi kwa wana wenu baada yenu mpaka wakati usio na kipimo.

9 "Nawe, Sulemani mwananguu, mjue[a] Mungu wa baba yako, umtumikie[b] kwa moyo kamili[c] na kwa nafsi yenye shangwe;[d] kwa maana Yehova anaichunguza mioyo yote,[e] naye anatambua kila mwelekeo wa fikira.[f] Ukimtafuta, ataacha umpate;[g] lakini ukimwacha,[h] atakutupa mbali milele.[i] **10** Ona, sasa, kwa maana Yehova mwenyewe amekuchagua wewe ujenge nyumba iwe patakatifu. Uwe hodari na utende."[j]

11 Na Daudi akampa Sulemani mwana wake ramani ya ujenzi[k] wa ukumbi[l] na ya nyumba zake na ya maghala[m] yake na madari[n] yake na ya vyumba vyake vya ndani vyenye giza na nyumba ya kifuniko cha upatanisho;[o] **12** ile ramani ya ujenzi ya kila kitu aliyoipata kwa kuongozwa na roho[p] kwa ajili ya nyua[q] za nyumba ya Yehova na ya vyumba vyote vya kulia chakula[r] pande zote, ya hazina za nyumba ya Mungu wa kweli na ya hazina za vitu vilivyofanywa kuwa vitakatifu;[s] **13** na kwa ajili ya migawanyo[t] ya makuhani na ya Walawi na kwa ajili ya kazi zote za utumishi wa nyumba ya Yehova na ya vyombo vyote vya utumishi wa nyumba ya Yehova; **14** ya dhahabu kulingana na uzito, dhahabu kwa ajili ya vyombo vyote vya utumishi mbalimbali, ya vyombo vyote vya fedha kulingana na uzito, ya vyombo[u] vyote vya utumishi mbalimbali; **15** na uzito kwa ajili ya vinara vya taa[v] vya dhahabu na taa zake za dhahabu, kulingana na uzito wa vinara mbalimbali vya taa na taa zake, na ya vinara vya fedha kulingana na uzito wa kinara cha taa na taa zake kulingana na utumishi wa vinara mbalimbali vya taa; **16** na dhahabu kulingana na uzito kwa ajili ya meza za mkate wa tabaka,[a] kwa ajili ya meza mbalimbali, na fedha kwa ajili ya meza za fedha; **17** na nyuma na mabakuli[b] na mitungi ya dhahabu safi, na ya mabakuli madogo ya dhahabu[c] kulingana na uzito wa mabakuli madogo mbalimbali, na ya mabakuli madogo ya fedha kulingana na uzito wa mabakuli madogo mbalimbali; **18** na kwa madhabahu ya uvumba[d] dhahabu safi kulingana na uzito na kwa ajili ya mfano wa gari,[e] yaani, wale makerubi[f] wa dhahabu kwa ajili ya kutandaza mabawa yao na kusitiri sanduku la agano la Yehova. **19** "Alitoa ufahamu kwa ajili ya kitu hicho chote kwa njia ya maandishi[g] kutoka kwa mkono wa Yehova juu yangu, kwa ajili ya kazi zote za ile ramani ya ujenzi."[h]

20 Naye Daudi akaendelea kumwambia Sulemani mwana wake: "Uwe hodari[i] na mwenye nguvu nawe utende. Usiogope[j] wala usiwe na hofu,[k] kwa maana Yehova Mungu, Mungu wangu, yuko pamoja nawe.[l] Hatakutupa[m] wala kukuacha mpaka itakapomalizika kazi yote ya utumishi wa nyumba ya Yehova. **21** Na tazama, hii ndiyo migawanyo ya makuhani[n] na ya Walawi[o] kwa ajili ya utumishi wote wa nyumba ya Mungu wa kweli; na kila mtu ambaye ni mwenye kupenda[p] na mwenye ustadi kwa ajili ya utumishi[q] wote yuko pamoja nawe katika kazi yote, na pia wakuu[r] na watu wote, kwa ajili ya maneno yako yote."

SURA 28

a Zb 9:10
Yer 9:24
Ebr 8:11
b Kum 10:12
c 1Fa 8:61
2Fa 20:3
Zb 101:2
d Zb 37:4
Zb 73:25
e 1Sa 16:7
1Nya 29:17
Met 17:3
Ufu 2:23
f Mwa 6:5
Kum 31:21
Zb 139:2
g 2Nya 15:2
Mt 7:7
Ebr 11:6
Yak 4:8
h 2Nya 15:2
Ezr 8:22
i Kum 31:17
Zb 73:27
Isa 1:28
Ebr 10:38
j 1Nya 22:16
k Ebr 8:5
l 2Nya 3:4
m 1Nya 26:24
n 1Fa 6:5
o Law 16:2
1Fa 6:19
p 2Sa 23:2
Ebr 8:5
q 1Fa 6:36
1Fa 7:12
r 1Nya 9:26
s 1Nya 26:20
t 1Nya 24:1
u 1Nya 9:29
v 2Nya 4:7

Safu ya 2

a 2Nya 4:8
2Nya 4:19
b 2Fa 25:15
c 1Fa 7:50
d 1Fa 7:48
e Zb 18:10
f Kut 25:20
1Sa 4:4
1Fa 6:23
Zb 80:1
g Kut 25:40
h 1Nya 28:11
i Yos 1:6
2Ko 5:6
j Kum 31:6
1Nya 22:13
k Yos 1:9
l Kum 31:8
Ro 8:31
m Yos 1:5
n 1Nya 24:1
o 1Nya 24:20
1Nya 25:1
p Kut 35:26
Kut 36:2
Zb 110:3
q Kut 36:1
r 1Nya 22:17
1Nya 28:1

29 Basi Daudi mfalme aka-
liambia kutaniko lote:[a]
"Sulemani mwanangu, ambaye
Mungu amemchagua,[b] ni mcha-
nga[c] na mwororo, lakini kazi ni
kubwa; kwa kuwa jumba hilo la
kifalme si la mwanadamu,[d] bali
ni la Yehova Mungu. **2** Nami
kulingana na nguvu zangu
zote,[e] nimetayarisha[f] kwa ajili
ya nyumba ya Mungu wangu
dhahabu[g] kwa ajili ya kazi ya
dhahabu, na fedha kwa ajili ya
kazi ya fedha, na shaba kwa aji-
li ya kazi ya shaba, chuma[h] kwa
ajili ya kazi ya chuma, na mbao[i]
kwa ajili ya kazi ya mbao; mawe
ya shohamu,[j] na mawe ya ku-
pangwa kwa saruji ngumu, na
mawe maridadi ya mviringo,
na kila jiwe la thamani, na mawe
ya alabasta kwa wingi sana.
3 Na kwa kuwa ninapendezwa[k]
na nyumba ya Mungu wangu,
bado kuna mali yangu ya pekee,[l]
dhahabu na fedha; naitoa kwa
ajili ya nyumba ya Mungu wa-
ngu, kuongezea vyote ambavyo
nimetayarisha kwa ajili ya hiyo
nyumba takatifu:[m] **4** talanta
elfu tatu za dhahabu, za dhaha-
bu ya Ofiri,[n] na talanta elfu saba
za fedha iliyosafishwa, kwa ajili
ya kufunika kuta za hizo nyu-
mba; **5** za dhahabu kwa ajili
ya kazi ya dhahabu, na za fe-
dha kwa ajili ya kazi ya fedha na
kwa ajili ya kazi yote ya kufa-
nywa kwa mkono wa mafundi.
Na ni nani anayejitolea kuuja-
za mkono wake leo kwa za-
wadi kwa ajili ya Yehova?"[o]
6 Na wakuu[p] wa nyumba za
ukoo wa baba[q] na wakuu[r] wa
makabila ya Israeli na wakuu
wa maelfu[s] na wa mamia[t] na
wakuu wa shughuli[u] za mfalme
wakajitolea. **7** Basi wakatoa
kwa ajili ya utumishi wa nyu-
mba ya Mungu wa kweli dha-
habu yenye thamani ya talanta
elfu tano na dariki elfu kumi
na fedha yenye thamani ya ta-
lanta elfu kumi na shaba yenye
thamani ya talanta kumi na
nane elfu na chuma yenye tha-
mani ya talanta mia moja elfu.[a]
8 Na watu wowote waliokuwa
na mawe yoyote wakayatoa
kwa ajili ya hazina ya nyumba
ya Yehova chini ya amri ya Ye-
hieli[b] Mgershoni.[c] **9** Na watu
wakashangilia kutokana na
matoleo yao ya hiari waliyotoa,
kwa maana walimtolea Yeho-
va matoleo ya hiari kwa moyo
kamili;[d] na hata Daudi mfalme
akashangilia kwa shangwe ku-
bwa.[e]
10 Basi Daudi akambariki[f]
Yehova mbele ya macho ya ku-
taniko[g] lote na Daudi akasema:
"Na ubarikiwe,[h] Ee Yehova, Mu-
ngu wa Israeli[i] baba yetu, kuto-
ka wakati usio na kipimo
mpaka wakati usio na kipimo.
11 Ee Yehova, ukuu[j] ni wako na
nguvu[k] na uzuri[l] na utukufu[m]
na heshima;[n] kwa maana kila
kitu mbinguni na duniani ni
chako.[o] Ufalme[p] ni wako, Ee Ye-
hova, Wewe unayejiinua kuwa
kichwa juu ya wote.[q] **12** Utaji-
ri[r] na utukufu[s] hutokana na
wewe, nawe unatawala[t] kila
kitu; na mkononi mwako mna
nguvu[u] na uwezo,[v] na mkono-
ni mwako mna uwezo wa kufa-
nya kuwa na ukuu[w] na kuwa-
pa wote nguvu.[x] **13** Na sasa,
Ee Mungu wetu, tunakushuku-
ru[y] na kulisifu[z] jina lako zuri.[a]
14 "Ingawa hivyo, mimi ni
nani,[b] na watu wangu ni nani,
hata tuwe na nguvu za kutoa
matoleo ya hiari hivi?[c] Kwa maa-
na kila kitu hutoka kwako,[d]

SURA 29

a 1Nya 28:8
b 1Fa 8:19
1Nya 28:5
c 1Fa 3:7
Met 4:3
d 2Nya 2:4
e Mhu 9:10
f 1Nya 22:3
g 1Nya 22:16
h 1Nya 22:14
i 1Nya 22:4
j Kut 28:9
k Zb 26:8
Zb 27:4
Zb 122:1
l 1Nya 21:24
Met 3:9
m 1Nya 22:5
1Nya 22:16
n Ayu 28:16
o Kut 35:5
p 1Nya 27:1
q 1Nya 23:11
r 1Nya 28:1
s Kut 18:25
1Nya 13:1
t Kum 1:15
1Nya 27:1
u 1Nya 27:25
1Nya 27:29
1Nya 27:31

Safu ya 2

a 2Ko 9:11
b 1Nya 26:22
c 1Nya 6:1
d 2Ko 9:7
e Mdo 20:35
f 2Nya 31:8
g 1Fa 8:14
2Nya 6:3
h 1Fa 8:15
i Mwa 32:28
Zb 68:35
j Zb 145:3
1Ti 1:17
k Mwa 17:1
Ufu 5:13
l 1Nya 29:13
Zb 71:8
m 1Sa 15:29
n 1Nya 16:27
Zb 8:1
o Zb 24:1
Zb 115:15
Isa 42:5
Yer 10:12
p Zb 103:19
Mt 6:10
q Ne 9:5
Zb 97:9
r Kum 8:18
Met 10:22
Flp 4:19
s 1Fa 3:13
Yoh 17:5
t 2Nya 20:6
u Met 18:10
Isa 40:26
v Kum 3:24
Efe 1:19
Ufu 15:3
w 2Nya 1:12
Zb 75:7
x 2Nya 16:9
Zb 18:32
Zb 28:8
Isa 40:29
1Pe 4:11
y Zb 105:1
z Zb 106:1
a Isa 63:14
b 2Sa 7:18
c Zb 115:1
Flp 2:13

d Zb 50:12.

nasi tumekupa kutoka katika mkono wako mwenyewe.
15 Kwa maana sisi ni wakaaji wageni mbele zako na wahamiaji[a] sawa na mababu zetu.
Siku zetu duniani[b] ni kama kivuli wala hakuna tumaini.
16 Ee Yehova, Mungu wetu, wingi huu wote ambao tumetayarisha ili kukujengea nyumba
kwa ajili ya jina lako takatifu,
umetoka mkononi mwako, nao
wote ni mali yako.[c] **17** Nami
ninajua vema, Ee Mungu wangu, kwamba wewe ni mchunguzaji wa moyo,[d] nawe unafurahia unyoofu.[e] Nami katika
unyoofu wa moyo wangu, nimetoa kwa hiari vitu hivi vyote, na sasa watu wako waliopo hapa nimefurahi kuona wakikutolea matoleo kwa hiari.
18 Ee Yehova, Mungu wa Abrahamu, Isaka na Israeli mababu zetu,[f] shika hili mpaka wakati usio na kipimo kama mwelekeo wa fikira za moyo wa watu wako,[g] na uelekeze moyo
wao kwako.[h] **19** Na Sulemani mwanangu umpe moyo kamili[i] ili ashike amri[j] zako, shuhuda[k] zako na masharti[l] yako, afanye kila jambo, na kulijenga jumba[m] hili la kifalme ambalo nimelifanyia matayarisho."[n]

20 Na Daudi akaendelea kuliambia kutaniko lote:[o] "Sasa mbarikini[p] Yehova, Mungu wenu."
Nalo kutaniko lote wakambariki Yehova, Mungu wa mababu zao, wakainama[q] na kumsujudia[r] Yehova na mfalme.
21 Nao wakaendelea kutoa dhabihu[s] kwa Yehova na kutoa matoleo ya kuteketezwa[t] kwa Yehova siku ya pili yake, ng'ombe-dume wachanga elfu moja, kondoo-dume elfu moja, wanakondoo dume elfu moja na matoleo yao ya kinywaji,[u] dhabihu nyingi sana kwa ajili ya Israeli wote.[a] **22** Nao wakaendelea kula na kunywa mbele za Yehova siku hiyo kwa shangwe kubwa;[b] nao kwa mara ya pili wakamfanya Sulemani mwana wa Daudi kuwa mfalme,[c] wakamtia mafuta kwa Yehova awe kiongozi[d] na pia Sadoki[e] awe kuhani. **23** Na Sulemani akaanza kuketi juu ya kiti cha ufalme cha Yehova[f] akiwa mfalme mahali pa Daudi baba yake, akafanikiwa,[g] na Israeli wote walikuwa wakimtii. **24** Nao wakuu[h] wote na wanaume wenye nguvu[i] na pia wana wote wa Mfalme Daudi,[j] wakajitiisha kwa Sulemani mfalme. **25** Na Yehova akaendelea kumfanya Sulemani kuwa mkuu zaidi[k] mbele ya macho ya Israeli wote na kuweka juu yake heshima ya kifalme ambayo haikuwa imepata kuwa juu ya mfalme yeyote kabla yake juu ya Israeli.[l]

26 Naye Daudi mwana wa Yese, akatawala juu ya Israeli yote;[m] **27** na siku alizotawala juu ya Israeli zilikuwa miaka 40.[n] Katika Hebroni alitawala miaka 7,[o] na katika Yerusalemu alitawala miaka 33.[p]
28 Mwishowe akafa mwenye umri mwema wa uzeeni,[q] ameshiba siku, utajiri[r] na utukufu;[s] na Sulemani mwana wake akaanza kutawala mahali pake.[t]
29 Na mambo ya Daudi mfalme, ya kwanza na ya mwisho, yameandikwa katika maneno ya Samweli mwonaji[u] na katika maneno ya nabii Nathani[v] na katika maneno ya Gadi[w] mwonaji, **30** pamoja na ufalme wake wote na nguvu zake na nyakati[x] ambazo zilikuwa zimepita juu yake na juu ya Israeli na juu ya falme zote za nchi.[y]

SURA 29

a Law 25:23
Ebr 11:13
b Ayu 14:2
Yak 4:14
c Zb 24:1
d 1Nya 28:9
e Met 11:20
Met 15:8
Mdo 24:16
Ebr 1:9
f Kut 3:6
g 1Nya 28:9
h Zb 10:17
Zb 86:11
2Th 2:17
i 1Fa 8:61
2Fa 20:3
Mk 12:30
j 1Fa 6:12
1Nya 28:7
k Kum 4:45
Kum 6:17
1Fa 2:3
l Kum 7:11
Kum 12:1
m 1Nya 29:1
n 1Nya 22:14
o 1Nya 28:8
p 1Nya 16:36
Zb 134:2
Zb 145:1
Efe 1:3
q Mwa 24:26
Kut 4:31
r 2Nya 7:3
Ufu 7:11
s 2Nya 7:4
Ezr 6:17
t Law 1:3
1Fa 8:64
u Law 23:13
Hes 15:5

Safu ya 2

a 1Fa 8:63
b Kum 12:7
2Nya 7:10
Ne 8:12
c 1Nya 23:1
d 1Fa 1:35
e 1Fa 2:35
f 1Nya 28:5
g 1Nya 22:11
h 1Nya 22:17
1Nya 28:21
i 1Nya 28:1
j 2Sa 3:2
1Nya 3:5
k 1Fa 3:12
2Nya 1:1
l 2Nya 1:12
Mhu 2:9
m 1Nya 18:14
Zb 78:71
n 2Sa 5:4
1Fa 2:11
o 2Sa 2:11
p 2Sa 5:5
q 1Fa 1:1
Met 16:31
r 1Nya 29:12
s Met 29:23
t 1Fa 2:1
1Fa 2:10
1Fa 2:12
u 1Sa 9:9
v 2Sa 7:2
2Sa 12:1
w 1Nya 21:9
x Da 2:21
y 1Fa 2:11

KITABU CHA PILI CHA

MAMBO YA NYAKATI

1 Naye Sulemani mwana wa Daudi akaendelea kupata nguvu katika ufalme wake,[a] na Yehova Mungu wake alikuwa pamoja naye,[b] akaendelea kumfanya kuwa mkuu zaidi.[c]

2 Na Sulemani akasema na Israeli wote, kwa wakuu wa maelfu[d] na wa mamia[e] na kwa waamuzi[f] na wakuu wote wa Israeli,[g] vichwa vya nyumba za ukoo wa upande wa baba.[h] **3** Kisha Sulemani na kutaniko lote pamoja naye wakaenda mahali pa juu palipokuwa katika Gibeoni;[i] kwa maana hapo ndipo lilipokuwa lile hema la mkutano[j] la Mungu wa kweli, ambalo Musa mtumishi[k] wa Yehova alitengeneza nyikani. **4** Hata hivyo, Daudi alikuwa amelileta sanduku[l] la Mungu wa kweli kutoka Kiriath-yearimu[m] mpaka mahali ambapo Daudi alikuwa amelitayarishia,[n] kwa maana alikuwa amelisimamishia hema katika Yerusalemu.[o] **5** Na ile madhabahu ya shaba[p] ambayo Bezaleli[q] mwana wa Uri mwana wa Huru[r] alikuwa ametengeneza ilikuwa imewekwa mbele ya maskani ya Yehova; na Sulemani na kutaniko wakatoa maombi yao mbele yake kama kawaida. **6** Kisha Sulemani akafanya matoleo hapo mbele za Yehova juu ya ile madhabahu ya shaba ya hema la mkutano, naye akatoa juu yake matoleo elfu moja ya kuteketezwa.[s]

7 Usiku huo Mungu akamtokea Sulemani na kumwambia: "Omba! Nikupe nini?"[t] **8** Ndipo Sulemani akamwambia Mungu: "Wewe Ndiye uliyemwonyesha Daudi baba yangu[a] fadhili kubwa zenye upendo na kunifanya niwe mfalme mahali pake.[b] **9** Sasa, Ee Yehova Mungu, acha ahadi yako kwa Daudi baba yangu itimie,[c] kwa maana wewe mwenyewe umenifanya kuwa mfalme[d] juu ya watu wengi sana kama chembe za mavumbi ya dunia.[e] **10** Sasa unipe hekima na ujuzi[f] ili nitoke mbele ya watu hawa na ili niingie ndani,[g] kwa maana ni nani anayeweza kuwahukumu hawa watu wako walio wengi?"[h]

11 Ndipo Mungu akamwambia Sulemani: "Kwa sababu jambo hili liko moyoni[i] mwako nawe hukuomba mali, utajiri wala heshima wala nafsi ya wale wanaokuchukia, wala hata hukuomba wingi wa siku,[j] bali unaomba hekima na ujuzi kwa ajili yako ili uwahukumu watu wangu ambao nimekufanya kuwa mfalme juu yao,[k] **12** unapewa hekima na ujuzi;[l] pia nitakupa mali na utajiri na heshima ambavyo hakuna mfalme yeyote aliyekutangulia amepata kuwa navyo,[m] wala baada yako hakuna yeyote atakayekuwa navyo."[n]

13 Basi Sulemani akatoka pale mahali pa juu palipokuwa katika Gibeoni,[o] kutoka mbele ya hema la mkutano,[p] akaja Yerusalemu, akaendelea kutawala juu ya Israeli.[q] **14** Na Sulemani akaendelea kukusanya magari na farasi wa vita hivi kwamba akawa na magari elfu moja na mia nne na farasi wa vita kumi na

SURA 1

a 1Fa 2:12
b 2Sa 7:12
c 1Fa 3:13
1Nya 29:25
Mhu 2:9
Mt 6:29
Mt 12:42
d Kut 18:25
e Kum 1:15
f 1Nya 23:4
1Nya 26:29
g 1Nya 28:1
h 1Nya 24:31
1Nya 27:1
i 1Fa 3:5
1Nya 16:39
1Nya 21:29
j Kut 40:2
Law 1:1
k Kum 34:5
Ebr 3:5
l 2Sa 6:2
m 1Nya 13:5
n 1Nya 15:1
o 1Nya 16:1
Zb 132:5
p Kut 38:1
q Kut 31:2
r 1Nya 2:20
s 1Fa 3:4
t 1Fa 3:5

Safu ya 2

a 2Sa 7:8
Zb 89:28
b 1Nya 28:5
c 2Sa 7:12
1Nya 17:25
1Nya 28:6
Zb 132:11
d 1Sa 2:7
1Fa 3:7
e Mwa 13:16
f 1Fa 3:9
Met 2:6
Met 3:13
Yak 1:5
g Hes 27:17
2Sa 5:2
h 1Fa 3:8
Zb 72:2
i 1Sa 16:7
1Nya 29:17
j 1Fa 3:11
k 1Fa 3:28
Met 14:8
l 1Fa 3:12
Zb 34:10
Efe 3:20
1Yo 5:15
m 1Nya 29:25
2Nya 9:22
Mhu 2:9
n 1Fa 3:13
o 1Fa 3:4
1Nya 16:39
1Nya 21:29
p Kut 40:2
q 1Fa 4:25

mbili elfu,[a] akawaweka katika majiji ya magari[b] na karibu na mfalme katika Yerusalemu.
15 Na mfalme akafanya fedha na dhahabu iliyomo Yerusalemu kuwa kama mawe;[c] naye akafanya mierezi iwe kama mikuyu[d] iliyoko Shefela[e] kwa wingi. **16** Na farasi wa Sulemani walisafirishwa kutoka Misri,[f] na wanabiashara wa mfalme wakawa wakichukua kundi la farasi kwa bei fulani.[g] **17** Nao wakawa wakipandisha na kusafirisha kwa ukawaida gari kutoka Misri kwa vipande 600 vya fedha na farasi kwa vipande 150; na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa wafalme wote wa Wahiti na wafalme wa Siria.[h] Walikuwa wakisafirisha vitu kupitia hao.

2 Basi Sulemani akatoa amri kwamba nyumba[i] ijengwe kwa ajili ya jina la Yehova[j] na nyumba kwa ajili ya ufalme wake.[k] **2** Na Sulemani akahesabu watu 70,000 wawe wabeba-mizigo na 80,000 wawe wachongaji wa mawe mlimani,[l] na 3,600 wawe waangalizi juu yao.[m] **3** Tena Sulemani akatuma watu kwa Hiramu[n] mfalme wa Tiro, akisema: "Kama ulivyomtendea Daudi[o] baba yangu, ulivyokuwa ukimletea mierezi ili ajijengee nyumba ya kukaa,— **4** tazama, ninajenga[p] nyumba kwa ajili ya jina[q] la Yehova Mungu wangu, ili niitakase[r] kwake, ili kufukiza mbele zake uvumba uliotiwa manukato,[s] pamoja na mkate[t] wa tabaka wa daima na matoleo ya kuteketezwa wakati wa asubuhi na jioni,[u] wakati wa sabato[v] na wakati wa miezi mipya[w] na kwenye majira ya sherehe[x] ya Yehova Mungu wetu. Hayo yatakuwa juu ya Israeli mpaka wakati usio na kipimo.[a] **5** Na nyumba nitakayoijenga itakuwa kuu,[b] kwa maana Mungu wetu ni mkuu kuliko miungu mingine yote.[c] **6** Na ni nani angeweza kuwa na nguvu za kumjengea nyumba?[d] Kwa maana mbingu na mbingu za mbingu hazimtoshi,[e] na mimi ni nani[f] kwamba nimjengee nyumba isipokuwa tu iwe ya kufukizia moshi wa uvumba mbele zake?[g] **7** Na sasa niletee mwanamume mwenye ujuzi ili afanye kazi kwa kutumia dhahabu na fedha na shaba[h] na chuma na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na uzi mwekundu na wa bluu, na anayejua jinsi ya kuchonga michoro, pamoja na wale walio na ustadi ambao wako pamoja nami katika Yuda na Yerusalemu, ambao Daudi baba yangu amewatayarisha.[i] **8** Nawe uniletee mierezi,[j] miberoshi[k] na misandali[l] kutoka Lebanoni,[m] kwa maana mimi najua vema kwamba watumishi wako wana uzoefu wa kukata miti ya Lebanoni,[n] (na, tazama, watumishi wangu wako pamoja na watumishi wako,) **9** ili kunitayarishia miti kwa hesabu kubwa, kwa maana ile nyumba nitakayoijenga itakuwa kuu, ndiyo, kuu ajabu. **10** Na, tazama! kwa wakusanyaji wa mbao, wakataji wa miti, ninatoa chakula kwa watumishi wako, kori 20,000 za ngano,[o] na kori 20,000 za shayiri, na bathi 20,000 za divai,[p] na bathi 20,000 za mafuta."

11 Ndipo Hiramu mfalme wa Tiro[q] akatoa neno katika maandishi, akalituma kwa Sulemani: "Kwa sababu Yehova aliwapenda[r] watu wake, amekufanya wewe kuwa mfalme juu yao."[s] **12** Na Hiramu aka-

SURA 1
a Kum 17:16; 1Fa 4:26
b 2Nya 8:6; 2Nya 9:25
c 1Fa 10:21
d 1Fa 10:27
e 2Nya 9:27; 2Nya 26:10
f 2Nya 9:28
g 1Fa 10:28
h 1Fa 10:29

SURA 2
i 1Fa 5:5
j Kum 12:11; 1Nya 22:10
k 1Fa 7:1
l 1Fa 5:15
m 1Fa 5:16; 1Fa 9:22; 2Nya 2:18
n 1Fa 5:1
o 2Sa 5:11; 1Nya 14:1
p 1Fa 8:19
q 2Nya 6:33
r 1Fa 8:64
s Kut 30:7
t Kut 25:30; Law 24:8; Mt 12:4
u Hes 28:4
v Kut 20:10; Hes 28:9
w Hes 10:10; Hes 28:11
x Law 23:4; 1Nya 23:31

Safu ya 2
a Law 23:14; Law 23:41
b 1Nya 29:1; Zb 68:29
c Kut 15:11; Zb 86:8; Zb 95:3; Zb 135:5
d Isa 66:1
e 1Fa 8:27; Mdo 17:24
f 2Sa 7:18; 1Nya 29:14
g Kum 12:6
h Kut 31:3; 1Fa 7:14
i 1Nya 22:15
j 1Fa 5:6
k 1Fa 5:8; 2Nya 3:5
l 1Fa 10:11
m 1Fa 5:14
n 1Fa 5:9
o 1Fa 5:11
p Ezr 7:22
q 1Fa 5:1; 1Fa 9:11; 1Nya 14:1
r Kum 7:8; Kum 33:3
s 1Fa 10:9

endelea kusema: “Abarikiwe
Yehova Mungu wa Israeli,[a] aliyezifanya mbingu na dunia,[b]
kwa sababu amempa Mfalme
Daudi mwana mwenye hekima, mwenye uzoefu katika busara na uelewaji,[c] atakayejenga
nyumba kwa ajili ya Yehova
na nyumba kwa ajili ya ufalme
wake.[d] **13** Na sasa namtuma
mtu mwenye ustadi, mwenye
uzoefu katika uelewaji, Hiramabi,[e] **14** mwana wa mwanamke wa wana wa Dani lakini
ambaye baba yake alikuwa mtu
wa Tiro, mwenye uzoefu, afanye mapambo ya dhahabu na
fedha, shaba,[f] chuma, mawe[g]
na miti, sufu iliyotiwa rangi
ya zambarau,[h] uzi wa bluu[i] na
kitambaa laini[j] na uzi mwekundu[k] na kuchonga kila na-
mna ya michoro[l] na kubuni kila
namna ya kitu[m] atakachoweza
kupewa pamoja na watu wako
wenye ustadi na watu wenye
ustadi wa bwana wangu Daudi
baba yako. **15** Na sasa ile ngano na shayiri, mafuta na divai
ambavyo bwana wangu ameahidi, na avilete kwa watumishi
wake.[n] **16** Nasi tutakata miti[o]
kutoka Lebanoni kulingana na
mahitaji yako yote,[p] nasi tutakuletea kama vyelezo kupitia
baharini[q] mpaka Yopa,[r] nawe
utaichukua na kuipeleka Yerusalemu.”

17 Ndipo Sulemani akawahesabu watu wote waliokuwa wa-
kaaji wageni, waliokuwa katika
nchi ya Israeli,[s] baada ya ile he-
sabu ya watu ambayo Daudi ali-
kuwa amechukua;[t] kukapatika-
na watu 153,600. **18** Kwa hiyo
akawafanya 70,000 kati yao
wawe wabeba-mizigo[u] na 80,000
wawe wachongaji[v] wa mawe
mlimani na waangalizi 3,600 wa
kuwafanya watu watumikie.[w]

SURA 2
a 1Fa 5:7
Zb 72:18
b Mwa 1:1
Zb 33:6
Mdo 17:24
Ufu 4:11
Ufu 10:6
c 2Nya 1:12
d 2Nya 2:1
e 1Fa 7:13
1Fa 7:40
2Nya 4:11
2Nya 4:16
Met 22:29
f 1Fa 7:14
g Kut 31:5
h Kut 39:1
i Kut 39:2
j Kut 39:5
k 2Nya 3:14
l Kut 39:6
m Kut 31:4
Kut 35:32
n 2Nya 2:10
o 1Fa 5:6
p 1Fa 5:8
q 1Fa 5:9
r Yos 19:46
Ezr 3:7
Mdo 9:36
s 1Fa 5:13
1Fa 5:14
2Nya 8:8
t 1Nya 22:2
u 1Fa 5:15
v 1Fa 5:17
1Fa 5:18
1Nya 22:15
w 1Fa 5:16

Safu ya 2

SURA 3
a 1Fa 6:14
1Nya 29:19
b Mwa 22:2
Mwa 22:14
c 2Sa 24:25
1Nya 21:18
d 2Sa 24:18
1Nya 21:22
e 1Fa 6:1
f 1Fa 6:2
g 1Fa 6:3
2Nya 29:7
h 1Fa 6:15
i 1Fa 6:22
1Nya 29:4
j 1Fa 6:29
k 1Fa 6:21
l 1Nya 29:2
1Nya 29:8
m 1Nya 29:4
n Kut 26:29
o Kut 26:1
1Fa 6:29
p Kut 26:33
1Fa 8:6
Ebr 9:3
Ebr 9:24
q 1Fa 6:20
r 1Nya 22:3

3 Mwishowe Sulemani akaanza kujenga nyumba ya Yehova[a] katika Yerusalemu juu
ya Mlima Moria,[b] ambapo Yehova alikuwa amemtokea Daudi baba yake,[c] mahali ambapo Daudi alikuwa ametayarisha kwenye uwanja wa kupuria
wa Ornani[d] Myebusi. **2** Basi
akaanza kujenga katika mwezi
wa pili, siku ya pili, katika mwaka wa nne wa utawala wake.[e]
3 Na vitu hivi Sulemani akaviweka kuwa msingi kwa ajili ya
kujenga nyumba ya Mungu wa
kweli, urefu wa kipimo cha mikono kulingana na kipimo cha
zamani ukiwa mikono 60, na
upana mikono 20.[f] **4** Na ukumbi[g] uliokuwa mbele ya huo
urefu ulikuwa mikono 20 mbele
ya upana wa nyumba, na kimo
chake kilikuwa 120; naye akafunika upande wa ndani kwa
dhahabu safi. **5** Na ile nyumba kuu[h] akaifunika kwa miberoshi, kisha akaifunika kwa
dhahabu nzuri,[i] halafu akaweka juu yake maumbo ya mtende[j]
na minyororo.[k] **6** Tena, akaitandaza nyumba kwa mawe ya
thamani kwa ajili ya uzuri;[l]
na dhahabu[m] ilikuwa dhahabu
ya kutoka katika nchi ya dhahabu. **7** Naye akafunika kwa
dhahabu ile nyumba, maboriti,
vizingiti na kuta zake na milango yake;[n] akachonga makerubi juu ya kuta.[o]

8 Naye akajenga nyumba ya Patakatifu Zaidi,[p] urefu wake
kuhusiana na upana wa nyumba ulikuwa mikono 20, na
upana wake ulikuwa mikono
20;[q] kisha akaifunika kwa dhahabu nzuri kiasi chake talanta
600. **9** Na uzito wa misumari[r]
ulikuwa shekeli 50 za dhahabu;
naye akavifunika vyumba vya
dari kwa dhahabu.

10 Kisha akatengeneza makerubi[a] wawili katika nyumba
ya Patakatifu Zaidi kwa kutumia ufundi wa kufanya mifano, akawafunika kwa dhahabu.[b] **11** Na urefu wa mabawa
ya wale makerubi[c] ulikuwa mikono 20, bawa moja la urefu wa mikono 5 lilifika kwenye ukuta wa nyumba ile, na
lile bawa lingine la urefu wa mikono 5 likiwa linafika kwenye bawa la yule kerubi mwingine.[d] **12** Na bawa la yule kerubi mmoja la urefu wa mikono 5 lilikuwa linafika kwenye ukuta wa nyumba ile, na lile bawa
lingine la mikono 5 lilishikana na bawa la yule kerubi mwingine.[e] **13** Mabawa ya hao makerubi yalikuwa yamenyooshwa urefu wa mikono 20; nao walikuwa wamesimama kwa miguu
yao, nyuso zao zikielekea upande wa ndani.

14 Tena akatengeneza pazia[f] la uzi wa bluu[g] na sufu iliyotiwa
rangi ya zambarau na uzi mwekundu na kitambaa laini, na kulipamba kwa makerubi juu yake.[h]

15 Kisha akatengeneza nguzo mbili[i] mbele ya nyumba ile,
urefu wa mikono 35, na kombe[j] lililokuwa juu ya kila moja lilikuwa na urefu wa mikono 5.
16 Tena, akatengeneza minyororo[k] yenye mtindo wa mkufu
na kuiweka juu ya vilele vya zile nguzo, akatengeneza makomamanga[l] mia moja na kuyaweka kwenye ile minyororo.
17 Naye akasimamisha zile nguzo mbele ya hekalu, moja
upande wa kuume na nyingine upande wa kushoto, kisha ile ya upande wa kuume akaiita jina Yakini na jina la ile ya upande
wa kushoto Boazi.[m]

SURA 3
a 1Fa 6:23
b 1Fa 6:28
c 1Fa 8:6
1Nya 28:18
2Nya 5:7
d 1Fa 6:24
e 1Fa 6:25
1Fa 6:27
f Mt 27:51
Ebr 10:20
g Kut 26:31
h Kut 36:35
i 1Fa 7:15
1Fa 7:21
2Fa 25:13
2Nya 4:12
Ufu 3:12
j 1Fa 7:16
2Fa 25:17
Yer 52:22
k 1Fa 7:17
l 1Fa 7:20
2Fa 25:17
2Nya 4:13
Yer 52:23
m 1Fa 7:21

Safu ya 2

SURA 4
a Kut 38:2
1Fa 8:22
2Fa 16:14
b Kut 20:26
c Kut 30:20
Kut 38:8
2Nya 4:6
d 1Fa 7:23
e 1Fa 6:18
f 1Fa 7:24
g Yer 52:20
h 1Fa 7:25
i 1Fa 6:35
j 1Fa 7:26
Eze 45:14
k 1Fa 7:39
l Law 9:14
m Law 1:9
n Kut 29:4

4 Kisha akatengeneza ile madhabahu ya shaba,[a] urefu wake ukiwa ni mikono 20,
na upana wake mikono 20, na kimo chake mikono 10.[b]

2 Naye akatengeneza bahari ya kuyeyushwa[c] urefu wa mikono 10 kutoka ukingo wake mmoja mpaka ukingo wake mwingine, ikiwa ni mviringo kuzunguka pande zote, na kimo
chake kilikuwa mikono 5, na kamba ya mikono 30 ingeweza kuizunguka pande zote.[d] **3** Na kulikuwa na mapambo yenye
umbo la kibuyu[e] chini yake kwenye mviringo wote, yakiizunguka, 10 katika kila urefu wa mkono mmoja, yakiizunguka ile bahari pande zote.[f] Yale mapambo
yenye umbo la kibuyu yalikuwa katika mistari miwili, yakiwa yamefanyizwa katika myeyusho wake. **4** Ilikuwa imesimama juu ya ng'ombe-dume kumi
na wawili,[g] watatu wakitazama kaskazini na watatu wakitazama magharibi na watatu wakitazama kusini na watatu wakitazama mashariki; na bahari ilikuwa juu yao, na sehemu zao
za nyuma zote zilielekea upande wa ndani.[h] **5** Na unene wake ulikuwa upana wa kiganja kimoja; na ukingo wake ulikuwa kama muundo wa ukingo
wa kikombe, ua la yungiyungi.[i] Nayo ikiwa kitu cha kuhifadhia, ingeweza kuchukua vipimo elfu tatu vya bathi.[j]

6 Tena akatengeneza beseni kumi, akaweka tano upande wa
kuume na tano upande wa kushoto,[k] ili kuoshea humo.[l] Wakawa wakioshea humo vitu vinavyohusiana na toleo la kuteketezwa.[m] Lakini ile bahari ilikuwa kwa ajili ya makuhani
kuogea humo.[n]

7 Kisha akatengeneza vinara vya taa[a] vya dhahabu, kumi vya muundo mmoja,[b] akaviweka katika hekalu, vitano upande wa kuume na vitano upande wa kushoto.[c]
8 Tena akatengeneza meza kumi, akaziweka katika hekalu, tano upande wa kuume na tano upande wa kushoto,[d] halafu akatengeneza mabakuli mia moja ya dhahabu.
9 Kisha akatengeneza ua[e] wa makuhani[f] na ule ua mkuu na milango ya ule ua,[g] akaifunika milango yake kwa shaba.
10 Naye akaweka ile bahari upande wa kuume, upande wa mashariki, kuelekea kusini.[h]
11 Mwishowe Hiramu akatengeneza makopo[i] na sepetu[j] na mabakuli.[k]

Basi Hiramu akamaliza kuifanya kazi aliyomfanyia Mfalme Sulemani kwenye nyumba ya Mungu wa kweli. **12** Zile nguzo[l] mbili na yale makombe ya mviringo[m] juu ya zile nguzo mbili na zile kamba mbili za nyavu[n] za kufunika yale makombe mawili ya mviringo yaliyokuwa juu ya zile nguzo **13** na yale makomamanga[o] mia nne kwa ajili ya zile kamba mbili za nyavu, mistari miwili ya makomamanga kwa kila kamba ya nyavu ili kufunika yale makombe mawili ya mviringo yaliyokuwa juu ya zile nguzo,[p] **14** na yale mabehewa[q] kumi na zile beseni[r] kumi juu ya yale mabehewa; **15** ile bahari[s] moja na wale ng'ombe-dume kumi na wawili walio chini yake,[t] **16** na makopo na sepetu[u] na nyuma[v] na vyombo[w] vyake vyote ambavyo Hiramabivu[x] alimtengenezea Mfalme Sulemani kwa ajili ya nyumba ya Yehova, vya shaba iliyong'arishwa. **17** Mfalme aliviyeyushia katika Wilaya ya Yordani katika ule udongo mzito kati ya Sukothi[a] na Sereda.[b] **18** Basi Sulemani akatengeneza vyombo hivyo vyote kwa wingi sana, kwa maana uzito wa ile shaba haukujulikana.[c]
19 Na Sulemani akatengeneza vyombo[d] vyote vilivyokuwa katika nyumba ya Mungu wa kweli na ile madhabahu ya dhahabu[e] na zile meza[f] zenye ule mkate wa wonyesho juu yake, **20** na vinara vya taa[g] na taa[h] zake za dhahabu safi, ili kuziwasha mbele ya chumba cha ndani kabisa[i] kulingana na kanuni; **21** na maua na taa na mikasi ya tambi,[j] ya dhahabu, (ilikuwa ndiyo dhahabu safi zaidi,) **22** na mikasi ya taa na mabakuli na vikombe na vyetezo, vya dhahabu safi,[k] na mwingilio wa nyumba,[l] milango yake ya ndani ya Patakatifu Zaidi na milango[m] ya nyumba ya hekalu, ya dhahabu.

5 Mwishowe kazi yote ambayo Sulemani alipaswa kufanya kwa ajili ya nyumba ya Yehova ikamalizika,[n] na Sulemani akaanza kuingiza vitu ambavyo Daudi baba yake alivifanya kuwa vitakatifu;[o] naye akaweka fedha na dhahabu na vyombo vyote katika hazina za nyumba ya Mungu wa kweli.[p]
2 Ndipo Sulemani akaanza kuwakusanya katika Yerusalemu wanaume wazee wa Israeli[q] na vichwa vyote vya makabila,[r] wakuu wa nyumba za ukoo wa upande wa baba[s] za wana wa Israeli, ili kulileta sanduku[t] la agano la Yehova kutoka[u] katika Jiji la Daudi,[v] yaani, Sayuni.[w] **3** Basi watu wote wa Israeli wakakusanyika kwa

SURA 4
a Kut 37:17 2Nya 4:20 Zek 4:2
b 1Nya 28:12
c Kut 40:24
d 2Nya 4:19
e Kut 27:9 Law 6:16
f 1Fa 6:36
g 1Fa 7:12
h 1Fa 7:39
i Kut 27:3 1Fa 7:45
j Kut 38:3 2Fa 25:14
k 1Fa 7:40
l 2Nya 3:17
m 1Fa 7:41
n 1Fa 7:17
o 1Fa 7:20
p 1Fa 7:42 Yer 52:22
q 1Fa 7:27 2Fa 25:16 Yer 52:17
r 1Fa 7:38
s 1Fa 7:23
t 1Fa 7:25
u 1Fa 7:40
v Kut 38:3
w Yer 52:19
x 2Nya 2:13

Safu ya 2
a Yos 13:24 Yos 13:27
b 1Fa 7:46
c 1Fa 7:47 1Nya 22:3 1Nya 22:14 Yer 52:20
d 2Fa 24:13 Ezr 1:7 Yer 28:3
e Kut 37:26 1Fa 7:48 2Nya 26:16 Ufu 8:3
f Kut 25:24 2Nya 4:8
g Kut 37:17 1Fa 7:49
h Kut 25:37
i 1Fa 6:16
j Kut 37:23
k 1Fa 7:50
l 1Fa 6:32
m 1Fa 6:34

SURA 5
n 1Fa 6:38 1Fa 7:51
o 1Nya 22:14
p 1Nya 26:26 Mt 23:17
q 1Fa 8:1
r Kum 1:13
s 1Nya 24:6 1Nya 24:31 2Nya 1:2
t Kut 25:10 Hes 10:33
u 2Sa 6:12 2Nya 1:4
v 2Sa 5:7 2Sa 5:9
w Zb 2:6 Isa 35:10 Mt 21:5

mfalme kwenye sherehe, ile ya mwezi wa saba.[a]

4 Basi wanaume wote wazee wa Israeli wakaja,[b] na Walawi wakaanza kulichukua Sanduku.[c] **5** Nao wakalipandisha Sanduku[d] na hema la mkutano[e] na vyombo vyote vitakatifu[f] vilivyokuwa katika hema. Makuhani Walawi wakavipandisha.[g] **6** Na Mfalme Sulemani na kusanyiko lote la Waisraeli, waliokutana naye kwa wakati uliowekwa mbele ya lile Sanduku walikuwa wakitoa dhabihu[h] za kondoo na ng'ombe ambao hawangeweza kuhesabiwa kwa sababu ya wingi. **7** Ndipo makuhani wakaliingiza sanduku la agano la Yehova mahali pake, ndani ya chumba cha ndani kabisa[i] cha nyumba, ndani ya Patakatifu Zaidi,[j] chini ya mabawa ya wale makerubi.[k] **8** Basi makerubi waliendelea kunyoosha mabawa yao juu ya mahali pa lile Sanduku, hivi kwamba makerubi walilifunika Sanduku na miti yake[l] kutoka juu.[m] **9** Lakini ile miti ilikuwa mirefu, hivi kwamba ncha za miti hiyo zilionekana katika Patakatifu mbele ya chumba cha ndani kabisa, lakini hazikuonekana nje, nayo iko hapo mpaka leo hii.[n] **10** Hamkuwa na chochote ndani ya lile Sanduku ila yale mabamba[o] mawili ambayo Musa aliwapa katika Horebu,[p] wakati Yehova alipofanya agano[q] na wana wa Israeli walipokuwa wakitoka Misri.[r]

11 Na ikawa kwamba makuhani walipoondoka mahali patakatifu (kwa maana makuhani wote waliopatikana walikuwa wamejitakasa[s]—hapakuwa na uhitaji wa kufuata ile migawanyo);[t] **12** na Walawi[u] waliokuwa waimbaji wa wote hawa, yaani, wa Asafu,[a] wa Hemani,[b] wa Yeduthuni[c] na wa wana wao na wa ndugu zao, waliovaa mavazi ya kitambaa laini pamoja na matoazi[d] na vinanda[e] na vinubi,[f] walikuwa wamesimama upande wa mashariki wa ile madhabahu na pamoja nao makuhani wenye kufikia hesabu ya 120 wakipiga tarumbeta;[g] **13** na ikawa kwamba mara tu wapiga-tarumbeta na waimbaji walipokuwa kama mtu mmoja[h] kwa kutokeza sauti moja isikike katika kumsifu na kumshukuru Yehova, na mara tu walipopaaza sauti kwa tarumbeta na kwa matoazi na kwa vyombo vya nyimbo[i] na kwa kumsifu[j] Yehova, "kwa maana yeye ni mwema,[k] kwa maana fadhili zake zenye upendo[l] ni za mpaka wakati usio na kipimo," nyumba ile ikajaa wingu,[m] nyumba ya Yehova,[n] **14** na makuhani hawakuweza kusimama ili kuhudumu kwa sababu ya lile wingu;[o] kwa maana utukufu[p] wa Yehova uliijaza nyumba ya Mungu wa kweli.

6 Ndipo Sulemani alipoSema:[q] "Yehova mwenyewe alisema kwamba atakaa katika giza zito;[r] **2** nami nimejenga nyumba ya makao yaliyoinuliwa[s] kwa ajili yako na mahali palipofanywa imara kwa ajili yako ili ukae humo mpaka wakati usio na kipimo."[t]

3 Kisha mfalme akageuza uso wake, akaanza kulibariki[u] kutaniko lote la Israeli, huku kutaniko lote la Israeli likiwa limesimama.[v] **4** Naye akaendelea kusema: "Na abarikiwe Yehova Mungu wa Israeli,[w] aliyesema kwa kinywa chake mwenyewe na Daudi baba ya-

SURA 5

a Law 23:34 1Fa 8:2 2Nya 7:8
b Yos 23:2
c Kut 25:14 Hes 4:15 1Nya 15:15
d Kut 37:1
e Kut 40:35 Hes 4:31
f Hes 4:15 1Fa 7:48
g 1Fa 8:4
h 2Sa 6:13 1Fa 8:5
i 1Fa 6:23
j 1Fa 6:20
k 1Fa 8:6
l Kut 25:14
m 1Fa 8:7
n 1Fa 8:8
o Kut 34:1 Kut 40:20 Kum 10:2
p Kum 4:15
q Kut 19:5 Kut 24:7 Kum 29:1 2Nya 6:11 Yer 31:32
r Kut 19:1
s Kut 19:10 Hes 8:21 2Nya 29:34 2Nya 30:24
t 1Nya 24:1 2Nya 35:4
u 1Nya 15:16 1Nya 16:4 1Nya 23:3 1Nya 25:1 2Nya 29:25 Ezr 3:10

Safu ya 2

a 1Nya 6:39 1Nya 15:19
b 1Nya 6:33 1Nya 15:17 1Nya 25:6
c 1Nya 16:41 1Nya 25:3
d 1Nya 15:16
e 2Sa 6:5
f 2Nya 9:11
g 1Nya 15:24
h Isa 52:8 Flp 1:27
i Zb 69:30
j Zb 84:4
k 1Nya 16:34 2Nya 7:10
l Kut 34:6
m 1Fa 8:10
n Kut 40:34 1Fa 8:11
o Kut 40:35 2Nya 7:2
p Kut 16:10 Eze 10:4 Ufu 21:23

SURA 6

q 1Fa 8:12
r Kut 20:21 Kum 4:11 Zb 97:2 Ebr 12:18
s 1Fa 8:13
t 2Nya 2:4 Zb 132:14
u 1Fa 8:55
v Ne 8:5
w Zb 41:13; Zb 145:10; Yak 3:9.

ngu[a] na kwa mikono yake mwenyewe ametimiza,[b] akisema,
5 ‘Kuanzia ile siku nilipowatoa watu wangu katika nchi
ya Misri, sikuchagua jiji kutoka
katika makabila yote ya Israeli ili kujenga nyumba kwa ajili
ya jina langu,[c] ili liwe hapo,
wala sikumchagua mwanadamu awe kiongozi juu ya watu
wangu Israeli.[d] **6** Bali nitachagua Yerusalemu[e] ili jina
langu liwe hapo, nami nitamchagua Daudi awe juu ya watu
wangu Israeli.’[f] **7** Na likawa
jambo lililo moyoni mwa Daudi baba yangu kujenga nyumba kwa ajili ya jina la Yehova Mungu wa Israeli.[g] **8** Lakini Yehova akamwambia Daudi
baba yangu, ‘Kwa sababu lilikuwa jambo lililo moyoni mwako kujenga nyumba kwa ajili ya jina langu, ulifanya vema,
kwa sababu lilikuwa jambo lililo moyoni mwako.[h] **9** Ila tu
wewe mwenyewe hutaijenga
nyumba hiyo,[i] bali mwana wako
atakayetoka katika viuno vyako ndiye atakayeijenga nyumba kwa ajili ya jina langu.’[j]
10 Na Yehova akatimiza neno
lake[k] alilokuwa amesema, ili nisimame mahali pa Daudi baba
yangu[l] na kuketi juu ya kiti
cha ufalme[m] cha Israeli, kama
Yehova alivyosema,[n] na ili nijenge nyumba kwa ajili ya jina
la Yehova Mungu wa Israeli,[o]
11 na ili niweke hapo lile Sandukuⁿ[p] ambamo mna agano la
Yehova alilofanya na wana wa
Israeli.”[q]

12 Naye akaanza kusimama
mbele ya madhabahu ya Yehova mbele ya kutaniko lote la
Israeli,[r] naye sasa akainyoosha
mikono yake.[s] **13** (Kwa maana Sulemani alikuwa amejenga jukwaa[t] la shaba na kuliweka katikati ya ua.[a] Urefu
wake ulikuwa mikono mitano,
na upana wake ulikuwa mikono
mitano, na kimo chake kilikuwa mikono mitatu; naye akaendelea kusimama juu yake.)
Naye akapiga magoti[b] mbele ya
kutaniko lote la Israeli, akainyoosha mikono yake kuelekea
mbinguni.[c] **14** Akaendelea
kusema: “Ee Yehova Mungu wa Israeli,[d] hakuna Mungu
kama wewe[e] mbinguni wala duniani, anayeshika agano[f] na fadhili zenye upendo kwa watumishi
wako wanaotembea mbele zako kwa moyo wao wote;[g]
15 wewe ambaye umemtimizia
mtumishi wako Daudi baba yangu yale uliyomwahidi,[h] hivi
kwamba ukatoa hiyo ahadi kwa
kinywa chako mwenyewe, na
kwa mkono wako mwenyewe
umetimiza kama ilivyo leo hii.[i]
16 Na sasa, Ee Yehova Mungu
wa Israeli, umtimizie mtumishi
wako Daudi baba yangu yale
uliyomwahidi, ukisema, ‘Mwanamume wa kwako hatakatiliwa mbali mbele zangu asiketi juu ya kiti cha ufalme cha
Israeli,[j] ikiwa tu wana wako[k]
wataangalia njia yao kwa kutembea katika sheria yangu[l]
kama vile ambavyo wewe umetembea mbele zangu.’[m] **17** Na
sasa, Ee Yehova Mungu wa Israeli,[n] acha ahadi[o] uliyomwahidi
mtumishi wako Daudi itimie.[p]

18 “Lakini, je, kweli Mungu
atakaa pamoja na wanadamu
duniani?[q] Tazama! Mbingu, ndiyo, mbingu za mbingu, haziwezi kukutosha;[r] sembuse basi,
nyumba hii ambayo nimeijenga![s] **19** Nawe ugeuke kuielekea sala ya mtumishi wako[t] na
ombi lake la kutaka kibali,[u] Ee
Yehova Mungu wangu, kwa kusikiliza kilio cha kusihi[v] na sala

SURA 6

a 1Nya 17:12
b 1Fa 8:15
Isa 55:11
c Kum 12:5
d 1Fa 8:16
e 2Nya 12:13
Zb 48:1
f 2Sa 7:8
1Nya 28:4
g 2Sa 7:2
1Fa 5:3
h 1Fa 8:18
2Ko 8:12
i 1Fa 8:19
j 2Sa 7:12
1Nya 17:4
k Yos 21:45
Ne 9:8
l 1Nya 29:23
m 1Nya 28:5
Ebr 1:8
n 1Nya 17:11
o 1Fa 8:20
p Kut 40:20
1Fa 8:9
2Nya 5:10
q 1Fa 8:21
r 1Fa 8:22
s Kut 9:33
Zb 28:2
1Ti 2:8
t Ne 8:4

Safu ya 2

a 1Fa 6:36
b 1Fa 8:54
Zb 95:6
Mdo 20:36
c Ezr 9:5
d 1Nya 29:10
e Kut 15:11
1Sa 2:2
Zb 86:8
Mik 7:18
f 1Fa 8:23
g Kum 7:9
2Fa 20:3
2Nya 16:9
Ne 1:5
h 1Fa 3:6
1Fa 6:12
i 2Sa 7:12
1Nya 22:10
j 1Fa 8:24
k 1Fa 6:12
l Zb 132:12
m Zb 26:3
n Kut 24:10
o 2Sa 7:25
Zb 119:49
p 1Fa 8:26
q 1Fa 8:27
Mdo 7:48
r 2Nya 2:6
Ne 9:6
Zb 148:13
Isa 40:12
Mdo 17:24
s 1Fa 8:27
Isa 66:1
t 2Nya 6:33
Zb 65:2
Da 9:18
u 2Nya 33:13
Zb 6:9
v Zb 5:2

ambayo mtumishi wako anatoa mbele zako,[a] **20** ili macho yako yafunguliwe[b] kuielekea nyumba hii mchana na usiku, kuelekea mahali ambapo ulisema utaweka jina lako,[c] kwa kusikiliza sala ambayo mtumishi wako anatoa kuelekea mahali hapa.[d] **21** Nawe usikilize kusihi kwa mtumishi[e] wako na kwa watu wako Israeli wanaposali kuelekea mahali hapa,[f] ili wewe usikie ukiwa katika makao yako, ukiwa mbinguni;[g] nawe usikie na kusamehe.[h]

22 "Mwanadamu akimtendea dhambi mwanadamu mwenzake[i] naye amlaani ili kumtia[j] chini ya wajibu wa laana hiyo, naye kwa kweli aingie katika laana hiyo mbele ya madhabahu yako katika nyumba hii,[k] **23** basi na usikie ukiwa mbinguni,[l] nawe utende[m] na kuwahukumu watumishi wako ili kumlipa yule mwovu kwa kuweka njia yake juu ya kichwa chake mwenyewe[n] na kwa kumtangaza mwadilifu[o] kuwa ni mwadilifu kwa kumpa kulingana na uadilifu wake mwenyewe.[p]

24 "Na watu wako Israeli wakishindwa mbele ya adui[q] kwa sababu waliendelea kukutendea dhambi,[r] nao kwa kweli warudi[s] na kulisifu jina lako[t] na kusali[u] na kutoa ombi la kutaka kibali mbele zako katika nyumba hii,[v] **25** basi na usikie ukiwa mbinguni,[w] nawe usamehe[x] dhambi ya watu wako Israeli, nawe uwarudishe[y] katika nchi uliyowapa wao na mababu zao.[z]

26 "Mbingu zikifungwa hivi kwamba hakuna mvua inayonyesha,[a] kwa sababu waliendelea kukutendea dhambi,[b] nao kwa kweli wasali kuelekea mahali hapa[c] na kulisifu jina lako,

SURA 6

a 1Fa 8:28
b 2Fa 19:16
Zb 33:18
Zb 34:15
c Kum 26:2
2Nya 6:9
Ne 1:9
d 1Fa 8:29
e Zb 5:1
f 2Nya 7:12
Da 6:10
g 2Fa 19:20
2Nya 30:27
h 2Nya 7:14
Mik 7:18
i 1Sa 2:25
j Ne 10:29
k 1Fa 8:31
l 2Nya 30:27
Zb 123:1
m 1Fa 8:32
n Hes 5:27
2Fa 9:26
Ayu 34:11
Met 1:31
Isa 3:11
Ga 6:7
o Kum 25:1
Zb 33:5
p Isa 3:10
Eze 18:20
q Law 26:17
Kum 28:25
Yos 7:8
r Yos 7:11
Amu 2:14
s Law 26:40
Ne 9:2
t Da 9:19
u Ezr 9:5
v 1Fa 8:33
Da 9:3
w Isa 57:15
x 1Fa 8:34
y Zb 106:47
z Mwa 13:15
Kut 6:8
a Yak 5:17
b Eze 14:13
c 1Fa 8:35

Safu ya 2

a Isa 9:13
Eze 18:30
b Zb 86:11
Zb 119:102
Isa 30:20
Isa 54:13
c Isa 30:21
Yer 6:16
Yer 42:3
d 1Fa 18:1
Zek 10:1
e 1Fa 8:36
f Ru 1:1
2Fa 6:25
2Nya 20:9
g Law 26:16
Kum 28:21
h Amo 4:9
Hag 2:17
i Kum 28:22
Amo 4:9
j Kum 28:38
Yoe 1:4
Yoe 2:25
k Zb 78:46
l Law 26:25
2Nya 12:2
2Nya 32:1
m 1Fa 8:37
n Eze 14:21
o 2Nya 20:6
Zb 91:15
p 2Nya 33:13

nao wageuke kutoka katika dhambi yao kwa sababu ulielendelea kuwatesa,[a] **27** basi na usikie ukiwa mbinguni, nawe usamehe dhambi ya watumishi wako, naam, ya watu wako Israeli, kwa sababu unawafundisha[b] kuhusu njia nzuri[c] wanayopaswa kutembea ndani yake; nawe unyeshe mvua[d] juu ya nchi yako ambayo umewapa watu wako kuwa fungu la urithi.[e]

28 "Njaa ikitokea[f] katika nchi, tauni[g] ikitokea, kukitokea joto lenye kuunguza,[h] ukungu,[i] nzige[j] na mende;[k] adui[l] zao wakiwazingira katika nchi ya malango yao[m]—pigo la namna yoyote na ugonjwa wa namna yoyote[n] — **29** sala yoyote,[o] ombi lolote la kutaka kibali[p] ambalo huenda likatolewa na mwanadamu au na watu wako wote Israeli,[q] kwa sababu wanajua kila mmoja wao pigo[r] lake na maumivu yake mwenyewe; wakati anaponyoosha mikono yake kuelekea nyumba hii,[s] **30** basi na usikie ukiwa mbinguni, makao yako,[t] nawe usamehe[u] na kumpa kila mmoja kulingana na njia zake zote,[v] kwa sababu unaujua moyo wake[w] (kwa maana ni wewe peke yako unayejua vema moyo wa wanadamu);[x] **31** kusudi wakuogope[y] kwa kutembea katika njia zako siku zote ambazo wako hai juu ya uso wa nchi ambayo uliwapa mababu zetu.[z]

32 "Na pia kwa mgeni ambaye si sehemu ya watu wako Israeli[a] na ambaye anatoka katika nchi ya mbali kwa saba-

q 1Fa 8:38; r Met 14:10; s Da 6:10; t Zb 33:14; Isa 63:15; Mt 23:22; u Zb 130:4; v Ayu 34:11; Zb 18:20; Ufu 2:23; w 1Nya 28:9; Yer 11:20; x 1Sa 16:7; 1Fa 8:39; Yer 17:10; y Kut 20:20; z Mwa 12:7; Yos 1:2; 1Fa 8:40; a Kut 12:48; Ru 1:16; Isa 56:3.

bu ya jina lako kuu[a] na mkono
wako wenye nguvu[b] na mko-
no wako ulionyooshwa,[c] nao
kwa kweli waje na kusali kue-
lekea nyumba hii,[d] **33** basi
na usikilize ukiwa mbinguni,
katika makao yako yaliyofa-
nywa imara,[e] nawe ufanye ku-
lingana na yote ambayo mge-
ni huyo anakuomba;[f] kusudi
watu wote wa dunia wapate ku-
lijua jina lako[g] nao wakuogo-
pe[h] kama vile watu wako Israeli
wanavyokuogopa, na ili wajue
kwamba jina lako limeitwa juu
ya nyumba hii ambayo nimei-
jenga.[i]

34 "Watu wako wakitoka
kwenda vitani[j] kupigana na
adui zao katika njia ambayo
unawatuma,[k] nao kwa kweli
wasali[l] kwako wakielekea upa-
nde wa jiji hili ambalo umeli-
chagua na nyumba ambayo ni-
meijenga kwa ajili ya jina lako,[m]
35 basi usikie ukiwa mbingu-
ni sala yao na ombi lao la ku-
taka kibali,[n] nawe ufanye huku-
mu kwa ajili yao.[o]

36 "Nao wakikutendea dha-
mbi[p] (kwa sababu hakuna mwa-
nadamu asiyetenda dhambi),[q]
nawe uwakasirikie na kuwatia
mkononi mwa adui, na wenye
kuwateka wawachukue mate-
ka na kuwapeleka katika nchi
ya adui iliyo mbali au iliyo ka-
ribu;[r] **37** nao warudiwe na fa-
hamu katika nchi ile ambayo
wamechukuliwa mateka, nao
hakika warudi na kutoa kwa-
ko ombi la kutaka kibali kati-
ka nchi ambayo wao ni mateka,[s]
wakisema, 'Tumetenda dha-
mbi,[t] tumekosa[u] nasi tumete-
nda uovu';[v] **38** nao kwa kwe-
li warudi kwako kwa moyo wao
wote[w] na kwa nafsi yao yote
katika nchi ambayo wao ni ma-
teka[x] wa wale waliowachukua

SURA 6

a Hes 9:14
Yos 9:27
Isa 56:6
Yoh 12:20
Mdo 8:27
b Kum 3:24
Yos 2:11
c 1Fa 8:42
d Mdo 2:10
e 2Nya 30:27
Zb 11:4
Zb 123:1
Ebr 9:24
f 1Fa 8:43
g Zb 22:27
Zb 46:10
h Yer 10:7
Ufu 14:7
i 1Fa 8:43
j Kum 20:1
2Nya 14:11
k Hes 31:2
Yos 8:1
Amu 1:2
1Sa 15:3
l 2Nya 14:11
2Nya 20:6
m 2Nya 3:2
n Zb 3:4
Da 9:17
o Isa 37:36
p 1Fa 8:46
q Zb 130:3
Mhu 7:20
Ro 3:23
r Law 26:34
Da 9:7
s 1Fa 8:47
t Law 26:40
Ne 1:6
Zb 106:6
u Da 9:5
v Ezr 9:6
Met 28:13
w Kum 30:2
1Sa 7:3
Yer 29:13
x Da 9:3

Safu ya 2

a 2Nya 33:7
Da 6:10
b 1Fa 8:48
c 2Nya 30:27
Zb 123:1
Ebr 9:24
d 1Fa 8:49
e Mwa 15:14
Yer 51:36
f Mik 7:18
g 2Nya 7:15
2Nya 16:9
Zb 11:4
Zb 34:15
Isa 37:17
h Zb 17:1
Zb 31:2
Zb 65:2
i Zb 132:8
j 1Nya 28:2
k Yos 3:13
1Sa 5:9
l Ne 9:25
Zb 65:4
m 1Fa 1:34
Zb 18:50
n Mdo 13:34

SURA 7

o 1Fa 8:54
p 1Fa 18:38
q Law 9:24
1Nya 21:26

mateka, nao kwa kweli wasa-
li kuelekea upande wa nchi yao
uliyowapa mababu zao na jiji
ambalo umelichagua[a] na nyu-
mba ambayo nimeijenga kwa
ajili ya jina lako;[b] **39** basi usi-
kie ukiwa mbinguni, katika ma-
makao yako yaliyofanywa imara,[c]
sala yao na maombi yao ya ku-
taka kibali,[d] nawe ufanye huku-
mu[e] kwa ajili yao na kuwasame-
he[f] watu wako ambao wameku-
tendea dhambi.

40 "Basi, tafadhali, Ee Mu-
ngu wangu, macho[g] yako ya-
funguliwe na masikio[h] yako ya-
sikilize sala inayohusu maha-
li hapa. **41** Na sasa usimame,[i]
Ee Yehova Mungu, uingie kati-
ka pumziko lako,[j] wewe pamo-
ja na Sanduku la nguvu zako.[k]
Makuhani wako, Ee Yehova Mu-
ngu, na wavikwe wokovu, nao
washikamanifu wako washa-
ngilie katika wema.[l] **42** Ee Ye-
hova Mungu, usiugeuze nyu-
ma uso wa mtiwa-mafuta wako.[m]
Ee uzikumbuke fadhili zenye
upendo kwa Daudi mtumishi
wako."[n]

7 Basi mara tu Sulemani ali-
pomaliza kusali,[o] moto uka-
shuka kutoka mbinguni,[p] uka-
teketeza lile toleo la kuteketez-
wa[q] na zile dhabihu, na utuku-
fu[r] wa Yehova ukaijaza nyumba
ile. **2** Na makuhani hawaku-
weza kuingia ndani ya nyumba
ya Yehova[s] kwa sababu utuku-
fu wa Yehova ulikuwa umeija-
za nyumba ya Yehova. **3** Na
wana wote wa Israeli walikuwa
wakitazama wakati moto uli-
poshuka na utukufu wa Yeho-
va ulipokuwa juu ya nyumba
ile, kisha wakainama[t] kifudifu-
di mara moja, juu ya sakafu

r Kut 40:34; 1Fa 8:11; s Kut 40:35; t Kut 4:31.

ya mawe, wakasujudu[a] na kumshukuru Yehova, "kwa maana yeye ni mwema,[b] kwa maana fadhili zake zenye upendo ni za mpaka wakati usio na kipimo."[c]

4 Na mfalme na watu wote walikuwa wakitoa dhabihu mbele za Yehova.[d] **5** Na Mfalme Sulemani akatoa dhabihu ya ng'ombe 22,000 na kondoo 120,000.[e] Hivyo ndivyo mfalme na watu wote walivyoizindua[f] nyumba ya Mungu wa kweli. **6** Na makuhani[g] walikuwa wamesimama katika vituo vyao vya kazi, na Walawi[h] wakiwa na vyombo vya nyimbo[i] kwa Yehova ambavyo Daudi[j] mfalme alikuwa amevitengeneza ili kumshukuru Yehova, "kwa maana fadhili zake zenye upendo ni za mpaka wakati usio na kipimo," wakati Daudi alipokuwa akitoa sifa kwa mkono wao; na makuhani walikuwa wakipiga kwa sauti kubwa zile tarumbeta[k] mbele zao, huku Israeli wote wakiwa wamesimama.

7 Kisha Sulemani akatakasa[l] sehemu ya katikati ya ua uliokuwa mbele ya nyumba ya Yehova, kwa sababu alitolea hapo yale matoleo ya kuteketezwa[m] na vile vipande vya mafuta vya dhabihu za ushirika, kwa maana madhabahu ya shaba[n] ambayo Sulemani alikuwa ametengeneza haikuweza kutoshea toleo la kuteketezwa na toleo la nafaka[o] na vipande vya mafuta.[p] **8** Na Sulemani akaifanya sherehe[q] hiyo wakati huo kwa siku saba, na Israeli wote pamoja naye,[r] kutaniko kubwa sana[s] kuanzia maingilio ya Hamathi[t] kushuka mpaka kwenye bonde la mto la Misri.[u] **9** Lakini katika siku ya nane wakafanya kusanyiko kuu,[v] kwa sababu kule kuzinduliwa kwa madhabahu walikuwa wamekufanya kwa siku saba na ile sherehe kwa siku saba. **10** Na katika siku ya 23 ya mwezi wa 7 akawaruhusu watu waende zao nyumbani kwao, wakiwa na shangwe[a] na kuchangamka moyoni kutokana na wema[b] ambao Yehova alikuwa amemtendea Daudi na Sulemani na Israeli watu wake.[c]

11 Hivyo Sulemani akaimaliza nyumba ya Yehova[d] na nyumba ya mfalme;[e] na kila jambo ambalo lilikuwa limeingia moyoni mwa Sulemani kufanya kuhusiana na nyumba ya Yehova na nyumba yake mwenyewe yeye alifanikiwa. **12** Sasa Yehova akamtokea[f] Sulemani wakati wa usiku na kumwambia: "Nimeisikia sala yako,[g] nami nimechagua[h] mahali hapa kwa ajili yangu mwenyewe ili pawe nyumba ya dhabihu.[i] **13** Ninapofunga mbingu ili mvua isinyeshe[j] nami ninapoamuru panzi waile nchi[k] nami nikileta tauni katikati ya watu wangu,[l] **14** na watu wangu[m] ambao jina langu limeitwa[n] juu yao wajinyenyekeze[o] na kusali[p] na kutafuta uso wangu[q] na wageuke kutoka katika njia zao mbaya,[r] basi mimi nitasikia nikiwa mbinguni[s] na kusamehe dhambi yao,[t] nami nitaiponya nchi yao.[u] **15** Sasa macho[v] yangu yatakuwa wazi na masikio[w] yangu yatasikiliza sala katika mahali hapa. **16** Na sasa naichagua[x] na kuitakasa nyumba hii ili jina langu[y] liwe hapo mpaka wakati usio na kipimo,[z] na macho yangu na moyo wangu vitakuwa hapo sikuzote.[a]

17 "Na wewe ukitembea mbele zangu, kama Daudi[b] baba yako alivyotembea, kwa kutenda kulingana na yote ambayo

SURA 7

a Zb 95:6
b Zb 31:19 Mt 19:17
c Ru 2:20 Yer 31:3 Omb 3:22
d 1Fa 8:62
e 1Fa 8:63
f Hes 7:10 2Nya 2:4 Ezr 6:16
g 2Nya 5:11
h 1Nya 23:5
i 1Nya 25:7
j 1Fa 10:12 Zb 138:8
k 2Nya 5:13
l 1Fa 8:64
m Law 1:3
n 2Nya 4:1
o Law 2:1
p Law 4:8
q Law 23:34 Kum 16:13
r 1Fa 8:65
s 2Nya 30:13
t Hes 34:8 2Fa 14:25
u Hes 34:5 2Fa 24:7 Isa 27:12
v Law 23:36 Kum 16:8 Ne 8:18

Safu ya 2

a Kum 12:7 Kum 16:15 Ne 8:10
b 2Nya 6:41
c 1Fa 8:66
d 1Fa 9:1
e Mhu 2:4
f 1Fa 9:2 2Nya 1:7
g 2Fa 20:5 Zb 66:19 Lu 1:13 Mdo 10:31 1Pe 3:12
h Kum 12:5 Zb 78:68
i Kum 12:6 2Nya 2:6
j 2Nya 6:26
k Kum 28:38
l Law 26:16 Hes 16:46 Eze 14:19
m Kut 19:5 Kum 32:9
n Hes 6:27 Isa 43:10 Isa 63:19
o Law 26:41 2Nya 33:12 Yak 4:10
p 2Nya 6:37
q Ho 5:15
r Kum 30:2 Met 28:13 Isa 55:7
s 2Nya 30:27
t 2Nya 6:39 Zb 103:3
u Zb 60:2
v 2Nya 16:9
w 2Nya 6:40
x Kum 12:21
y 1Fa 8:16
z 1Fa 9:3
a 2Nya 6:20
b 1Fa 9:4 Zb 26:3

nimekuamuru,[a] nawe uyashike
masharti[b] yangu na maamuzi
yangu ya hukumu[c] **18** mimi
pia nitakifanya imara kiti cha
ufalme wako,[d] kama nilivyofa-
nya agano pamoja na Daudi
baba yako,[e] nikisema, 'Hakuna
mwanamume wa kwako ataka-
yekatiliwa mbali asitawale juu
ya Israeli.'[f] **19** Lakini mkige-
uka[g] nyuma na kwa kweli mzi-
ache kanuni zangu[h] na amri
zangu[i] ambazo nimeweka mbe-
le yenu, nanyi kwa kweli mwe-
nde kuitumikia miungu mingi-
ne[j] na kuiinamia,[k] **20** mimi
pia nitawang'oa kutoka katika
nchi yangu ambayo nimewapa;[l]
na nyumba hii ambayo nimei-
takasa[m] kwa ajili ya jina langu,
nitaitupilia mbali kutoka mbe-
le za uso wangu,[n] nami nitaifa-
nya kuwa neno la kimethali[o] na
shutuma kati ya vikundi vyote
vya watu.[p] **21** Na nyumba hii
iliyokuwa marundo ya mabo-
moko,[q] kila mtu anayepita ka-
ndo yake atatazama kwa msha-
ngao[r] na kwa hakika aseme,
'Kwa sababu gani Yehova ali-
tendea hivi nchi hii na nyumba
hii?'[s] **22** Nao watasema, 'Ni
kwa sababu walimwacha Yeho-
va[t] Mungu wa mababu zao, ali-
yekuwa amewatoa katika nchi
ya Misri,[u] nao wakashikamana
na miungu mingine[v] na kuiina-
mia na kuitumikia.[w] Ndiyo sa-
babu alileta juu yao msiba huu
wote.'"[x]

8 Na ikawa kwamba mwisho-
ni mwa miaka 20,[y] muda
ambao Sulemani alitumia ku-
jenga ile nyumba ya Yehova[z]
na nyumba yake mwenyewe,[a]
2 yale majiji ambayo Hira-
mu[b] alikuwa amempa Sulemani
—Sulemani aliyajenga upya
na kuwakalisha humo wana wa
Israeli. **3** Na zaidi ya hayo,

SURA 7

a Kum 4:40
b Kum 12:1
c Kum 4:5
d 2Sa 7:13
e Zb 89:28
f 1Fa 9:5
g Ebr 10:38
h Law 26:15
Zb 73:27
i Kum 28:15
j Yos 23:16
k Kut 20:5
1Fa 9:6
l Kum 4:26
2Fa 17:20
m 1Fa 9:7
n 2Fa 25:9
o Kum 28:37
Yer 24:9
p Zb 44:14
q 1Fa 9:8
2Fa 25:9
Yer 7:4
r 2Nya 29:8
Yer 19:8
Da 9:12
s Kum 29:24
Yer 22:8
t 2Nya 15:2
Zb 73:27
u Kut 12:51
Kum 29:25
v Zb 115:8
Isa 2:8
Yer 2:11
Yer 10:14
w 1Fa 9:9
x Kum 4:26
2Nya 36:17
Yer 22:9

SURA 8

y 1Fa 9:10
z 1Fa 6:37
1Fa 6:38
a 1Fa 7:1
b 2Sa 5:11
1Fa 5:2

Safu ya 2

a 1Fa 9:19
b 2Sa 8:9
2Fa 14:28
c Yos 16:5
1Nya 7:24
d Yos 16:3
1Fa 9:17
e Hes 32:17
Kum 28:52
2Fa 10:2
2Nya 12:4
f Kum 3:5
g Yos 19:44
1Fa 9:18
h 1Fa 4:26
i 1Fa 9:19
j Mhu 2:10
k Amu 3:3
1Fa 9:19
l Mwa 15:20
Kum 7:1
1Fa 11:1
2Fa 7:6
m Mwa 15:21
n Kut 34:11
o Kut 23:23
p Hes 13:29
q 1Fa 9:20
r Yos 15:63
Yos 17:12
Zb 106:34
s 1Fa 9:21

Sulemani akaenda Hamath-
soba na kulishinda. **4** Ndi-
po akajenga upya Tadmori ka-
tika nyika na majiji yote ye-
nye maghala[a] aliyokuwa ameje-
nga katika Hamathi.[b] **5** Naye
akajenga Beth-horoni ya Juu[c]
na Beth-horoni ya Chini,[d] maji-
ji yenye ngome yaliyo na kuta,[e]
milango na mapingo,[f] **6** na
Baalathi[g] na majiji yote yenye
maghala yaliyokuwa yameku-
wa ya Sulemani na majiji yote
ya magari[h] na majiji ya wa-
panda-farasi[i] na kila kitu che-
nye kutamanika cha Sulemani[j]
ambacho alikuwa ametamani
kukijenga katika Yerusalemu
na katika Lebanoni[k] na katika
nchi yote ya mamlaka yake.

7 Na watu wote waliokuwa
wameachwa wa Wahiti[l] na Waa-
mori[m] na Waperizi[n] na Wahivi[o]
na Wayebusi,[p] ambao hawaku-
wa sehemu ya Israeli,[q] **8** ku-
toka kwa wana wao waliooku-
wa wameachwa baada yao kati-
ka nchi, ambao wana wa Israeli
hawakuwaangamiza,[r] Sulema-
ni akaendelea kuwaandikisha[s]
kwa ajili ya kazi ya kulazimi-
shwa mpaka leo hii.[t] **9** Laki-
ni Sulemani hakumfanya ye-
yote kati ya wana wa Israeli
kuwa mtumwa kwa ajili ya
kazi yake;[u] kwa maana hao
walikuwa mashujaa wa vita[v]
na wakuu wa maamiri wake
wasaidizi na wakuu wa wa-
endesha-magari[w] wake na wa-
kuu wa wapanda-farasi[x] wake.
10 Hawa ndio waliokuwa wa-
kuu wa wasaidizi[y] wa Mfalme
Sulemani, watu 250, wasimami-
zi wa kazi juu ya watu.[z]

11 Na Sulemani akamtoa bi-
nti ya Farao[a] katika Jiji la

t Yos 16:10; 2Nya 2:17; u Kut 19:6; Law 25:39; v 1Sa 8:12; w 1Sa 8:11; x 1Fa 9:22; y 1Fa 5:16; z 1Fa 9:23; a 1Fa 3:1.

Daudi,[a] akampeleka katika
nyumba aliyokuwa amemjen-
gea,[b] kwa maana alisema:
"Ingawa yeye ni mke wangu,
asikae katika nyumba ya Daudi
mfalme wa Israeli, kwa maana
mahali ambapo sanduku la Ye-
hova limeletwa ni patakatifu."[c]
12 Ndipo wakati huo Sule-
mani akamtolea Yehova dhabi-
hu[d] za kuteketezwa juu ya ile
madhabahu[e] ya Yehova amba-
yo alikuwa amejenga mbele
ya ukumbi,[f] **13** kama destu-
ri ya kila siku[g] ili kutoa mato-
leo kulingana na amri ya Musa
kwa ajili ya sabato[h] na kwa aji-
li ya miezi mipya[i] na kwa aji-
li ya sherehe rasmi[j] mara tatu
kwa mwaka,[k] kwenye sherehe
ya keki zisizo na chachu[l] na
kwenye sherehe ya majuma[m] na
kwenye sherehe ya vibanda.[n]
14 Tena akaweka ile migawa-
nyo[o] ya makuhani juu ya utu-
mishi wao kulingana na kanuni
ya Daudi baba yake,[p] na Wala-
wi[q] katika vituo vyao vya kazi,
ili kusifu[r] na kuhudumu[s] mbele
ya makuhani kama desturi ya
kila siku,[t] na watunza-malango
katika migawanyo yao kwa aji-
li ya malango mbalimbali,[u] kwa
maana hivyo ndivyo ilivyoku-
wa amri ya Daudi mtu wa Mu-
ngu wa kweli. **15** Nao hawa-
kuiacha amri ya mfalme kwa
makuhani na Walawi kuhusu
jambo lolote na kuhusu akiba
ya mali.[v] **16** Basi kazi yote ya
Sulemani ilikuwa katika hali ili-
yotayarishwa[w] kuanzia siku ya
kuweka msingi wa nyumba ya
Yehova mpaka ilipomalizika.[x]
Basi nyumba ya Yehova ikama-
lizika.[y]
17 Wakati huo ndipo Sule-
mani alipoenda Esion-geberi[z]
na Elothi[a] kando ya bahari ka-
tika nchi ya Edomu.[b] **18** Naye
Hiramu[a] kupitia watumishi
wake akampelekea kwa ukawa-
ida meli na watumishi wenye
ujuzi wa bahari,[b] nao wakawa
wakienda Ofiri[c] pamoja na wa-
tumishi wa Sulemani na kuchu-
kua kutoka huko talanta 450[d]
za dhahabu,[e] wakamletea Mfa-
lme Sulemani.[f]
9 Na malkia wa Sheba[g] aka-
sikia habari za Sulemani,
naye akaja Yerusalemu ili ku-
mjaribu Sulemani kwa maswa-
li yenye kutatanisha,[h] pamo-
ja na msafara wenye kuvutia
sana na ngamia[i] wenye kuchu-
kua mafuta ya zeri,[j] na dha-
habu[k] nyingi sana, na mawe
ya thamani.[l] Mwishowe akain-
gia kwa Sulemani na kumwa-
mbia kila jambo lililokuwa mo-
yoni mwake.[m] **2** Naye Sule-
mani akamwambia mambo
yake yote,[n] hakuna jambo lo-
lote lililofichwa kwa Sulema-
ni ambalo hakumwambia yule
malkia.[o]
3 Malkia wa Sheba alipo-
ona hekima[p] ya Sulemani na
ile nyumba aliyokuwa ameje-
nga,[q] **4** na chakula cha meza[r]
yake na kuketi kwa watumi-
shi wake na utumishi wa me-
zani wa wale wenye kumhudu-
mia na mavazi[s] yao na wanywe-
shaji[t] wake na mavazi yao, na
dhabihu zake za kuteketezwa[u]
alizotoa kwa ukawaida katika
nyumba ya Yehova,[v] basi hai-
kubaki roho yoyote ndani yake.
5 Kwa hiyo akamwambia mfa-
lme: "Ni la kweli neno lile nililo-
sikia katika nchi yangu kuhusu
mambo yako na kuhusu hekima
yako.[w] **6** Nami sikuyaamini[x]
maneno yao mpaka nilipokuja
ili nijionee kwa macho yangu

SURA 8
a 1Fa 9:24
b 1Fa 7:8
c Kut 29:43
d Law 1:3
e 2Nya 4:1
f 1Fa 6:3
Eze 8:16
g Kut 29:38
Hes 28:3
h Hes 28:9
i Hes 10:10
Hes 28:11
j Kut 23:14
Law 23:4
k Kum 16:16
l Law 23:6
m Law 23:16
Mdo 2:1
n Law 23:34
o 1Nya 24:1
2Nya 5:11
Lu 1:5
p 1Nya 23:3
q 1Nya 15:16
1Nya 25:1
r 1Nya 6:31
1Nya 16:42
s 1Nya 16:4
1Nya 24:31
t 2Nya 35:10
u 1Nya 9:17
1Nya 26:1
v 1Nya 9:29
1Nya 26:20
w 1Fa 5:18
x 1Fa 6:1
1Fa 6:7
y 1Fa 7:51
z Hes 33:35
1Fa 22:48
2Nya 20:36
a Kum 2:8
2Fa 14:22
2Fa 16:6
b Mwa 36:1
1Fa 9:26

Safu ya 2
a 2Sa 5:11
b 1Fa 9:27
c 1Fa 22:48
Zb 45:9
d Kut 38:24
e 1Fa 10:22
2Nya 9:13
f Mhu 2:8

SURA 9
g 1Fa 10:1
Isa 60:6
Lu 11:31
h Mt 12:42
Mt 22:46
i Mwa 24:10
Isa 60:6
j 2Fa 20:13
k Zb 72:15
l 1Fa 10:2
Mt 17:8
m Mt 12:34
n 1Fa 10:3
Met 1:5
o 1Fa 3:12
p 1Fa 3:28
1Fa 10:4
Mhu 12:9
q 1Fa 6:1
2Nya 3:1
2Nya 4:11
r 1Fa 4:22
s 1Fa 10:5
t Ne 1:11
u Law 1:3

v 2Nya 8:13; w 1Fa 10:6; Mt 11:19; x Met 14:15; Lu 11:31.

mwenyewe;[a] na, tazama! sikuambiwa hata nusu ya wingi wa
hekima yako.[b] Umezidi ile habari niliyosikia.[c] **7** Watu wako
ni wenye furaha,[d] na ni wenye
furaha hawa watumishi wako
wanaosimama mbele yako daima na kuisikiliza hekima yako.[e]
8 Na abarikiwe Yehova Mungu wako,[f] ambaye amependezwa[g] nawe kwa kukuweka juu
ya kiti chake cha ufalme[h] uwe
mfalme kwa ajili ya Yehova Mungu wako;[i] kwa sababu Mungu
wako alipenda[j] Israeli, ili kuisimamisha mpaka wakati usio
na kipimo, hivi kwamba akakuweka juu yao uwe mfalme[k] ili
utende uamuzi wa hukumu[l] na
uadilifu."[m]

9 Ndipo akampa mfalme talanta 120 za dhahabu,[n] na mafuta ya zeri[o] kwa wingi sana, na
mawe ya thamani;[p] na kulikuwa hakujapata kuwa na mafuta ya zeri kama yale ambayo
malkia wa Sheba alimpa Mfalme Sulemani.[q]

10 Na zaidi ya hayo, watumishi wa Hiramu[r] na watumishi
wa Sulemani walioleta dhahabu[s] kutoka Ofiri walileta mbao
za misandali[t] na mawe ya thamani.[u] **11** Na mfalme akatengeneza kwa zile mbao za misandali ngazi[v] kwa ajili ya nyumba ya Yehova na kwa ajili ya
nyumba ya mfalme[w] na pia vinubi[x] na vinanda[y] vya waimbaji,[z] na vitu kama hivyo havikuwa vimepata kuonekana kabla
ya hapo katika nchi ya Yuda.

12 Na Mfalme Sulemani akampa malkia[a] wa Sheba vyote vilivyompendeza, ambavyo aliomba, zaidi ya thamani ya vitu
alivyomletea mfalme. Basi akageuka, akaenda katika nchi
yake, yeye pamoja na watumishi wake.[b]

SURA 9

a 1Fa 10:7
Yoh 20:25
b Mhu 1:16
c 1Fa 4:31
1Fa 4:34
2Nya 1:12
d Met 3:13
Met 8:34
e 1Fa 10:8
f 1Fa 5:7
Zb 72:18
g 2Sa 15:25
Zb 18:19
h 1Nya 29:23
i 1Fa 10:9
j Kum 7:8
2Nya 2:11
k Yoh 1:49
l 2Sa 8:15
1Fa 3:9
Isa 9:7
m 2Sa 23:3
Zb 72:2
Isa 11:4
n 1Fa 9:14
Zb 72:10
o Mwa 43:11
p Met 20:15
q 1Fa 10:10
r 1Fa 9:27
s 1Fa 10:22
2Nya 8:18
Zb 72:10
t 1Fa 10:11
u 2Nya 3:6
v 1Fa 6:8
w 1Fa 7:1
x 1Fa 10:12
1Nya 25:1
Zb 92:3
Zb 150:3
y 2Sa 6:5
1Nya 23:5
z 1Nya 9:33
2Nya 5:12
a 1Fa 10:1
Met 11:25
Mt 12:42
Lu 6:38
Lu 11:31
b 1Fa 10:13

Safu ya 2

a 1Fa 10:14
2Nya 1:15
Zb 68:29
Zb 72:15
b Mwa 37:28
1Fa 10:15
Isa 23:2
Isa 45:14
c Zb 72:10
Yer 25:24
d 2Nya 12:9
e 1Fa 10:16
f 1Fa 10:17
g 1Fa 7:2
h 1Fa 10:18
i Mwa 49:9
Met 28:1
Ufu 5:5
j 1Fa 10:19
k Hes 23:24
l 1Fa 10:20
m Est 1:7
n 1Fa 10:21
o 1Fa 7:2

13 Na uzito wa dhahabu iliyoletwa kwa Sulemani katika mwaka mmoja ulijumlika
kuwa talanta 666 za dhahabu,[a]
14 zaidi ya zile zilizoletwa na
wasafiri na wanabiashara[b] waliokuwa wakileta na wafalme
wote wa Waarabu[c] na magavana wa nchi waliokuwa wakimletea Sulemani dhahabu na fedha.

15 Na Mfalme Sulemani akatengeneza ngao kubwa mia mbili za dhahabu iliyochanganywa[d] (akaweka shekeli mia sita za dhahabu iliyochanganywa kwenye kila ngao kubwa),[e] **16** na ngao ndogo mia
tatu za dhahabu iliyochanganywa (akaweka mina tatu za
dhahabu kwenye kila ngao ndogo).[f] Kisha mfalme akaziweka
katika Nyumba ya Msitu wa Lebanoni.[g]

17 Tena mfalme akatengeneza kiti kikubwa cha ufalme cha
pembe za tembo na kukifunika
kwa dhahabu safi.[h] **18** Na kulikuwa na vipandio sita vilivyoelekea kwenye kile kiti cha ufalme, na kulikuwa na kiti cha miguu cha dhahabu kwenye kile
kiti cha ufalme, (vilikuwa vimeunganishwa), na kulikuwa na
mikono ya kiti upande huu na
upande ule kando ya mahali pa
kuketi, na simba[i] wawili walisimama kando ya ile mikono ya
kiti.[j] **19** Na kulikuwa na simba[k] kumi na wawili waliosimama hapo juu ya vile vipandio
sita, upande huu na upande ule.
Hakuna ufalme mwingine wowote uliokuwa na kiti kilichotengenezwa hivyo.[l] **20** Na vyombo[m] vyote vya kunywea vya
Mfalme Sulemani vilikuwa vya
dhahabu,[n] na vyombo vyote
vya Nyumba ya Msitu wa Lebanoni[o] vilikuwa vya dhahabu

safi. Hapakuwa na kitu chochote cha fedha; haikuhesabiwa
kuwa kitu[a] katika siku za Sulemani. **21** Kwa maana meli za
mfalme zilikuwa zikienda Tarshishi[b] pamoja na watumishi wa
Hiramu.[c] Mara moja kila miaka
mitatu meli za Tarshishi zilikuja, zikiwa zimebeba dhahabu na
fedha,[d] pembe za tembo,[e] na sokwe na tausi.[f]

22 Basi Mfalme Sulemani
alikuwa mkuu katika utajiri[g]
na hekima[h] kuliko wafalme wengine wote wa dunia. **23** Na
wafalme wote wa dunia walikuwa wakiutafuta[i] uso wa Sulemani ili wasikie hekima[j] yake,
ambayo Mungu wa kweli alikuwa ametia moyoni mwake.[k]
24 Nao walikuwa wakileta kila
mmoja zawadi yake,[l] vyombo
vya fedha na vyombo vya dhahabu[m] na mavazi,[n] silaha na mafuta ya zeri, farasi na nyumbu
kama kawaida ya kila mwaka.[o]
25 Na Sulemani akawa na vibanda elfu nne vya farasi[p] na
magari na farasi[q] wa vita kumi
na mbili elfu, naye akaviweka vitu hivyo katika majiji ya
magari[r] na karibu na mfalme
katika Yerusalemu. **26** Naye
akawa mtawala juu ya wafalme wote kuanzia ule Mto hadi
kwenye nchi ya Wafilisti na
hadi kwenye mpaka wa Misri.[s] **27** Tena mfalme akaifanya fedha iliyomo Yerusalemu
kuwa kama mawe; naye akaifanya mierezi iwe kama mikuyu[t] iliyoko Shefela[u] kwa wingi.[v]
28 Na kulikuwa na wale waliomletea Sulemani farasi[w] kutoka Misri[x] na kutoka katika nchi
nyingine zote.

29 Na mambo mengine ya
Sulemani,[y] ya kwanza na ya
mwisho, je, hayakuandikwa
kati ya maneno ya Nathani[z]
nabii na katika unabii wa Ahiya[a] Mshilo,[b] na katika kumbukumbu ya maono ya Ido[c]
mwonaji kumhusu Yeroboamu[d]
mwana wa Nebati?[e] **30** Na Sulemani akaendelea kutawala
katika Yerusalemu juu ya Israeli yote kwa miaka 40. **31** Mwishowe Sulemani akalala pamoja na mababu zake. Basi wakamzika katika Jiji la Daudi baba
yake;[f] na Rehoboamu[g] mwana
wake akaanza kutawala mahali
pake.[h]

10 Na Rehoboamu[i] akaenda
Shekemu,[j] kwa maana
Waisraeli wote walikuja Shekemu ili kumfanya kuwa mfalme.
2 Na ikawa kwamba mara tu
Yeroboamu[k] mwana wa Nebati aliposikia habari hizo alipokuwa angali Misri,[l] (kwa maana alikuwa amekimbia kwa
sababu ya Sulemani mfalme,)
Yeroboamu akarudi mara moja
kutoka Misri.[m] **3** Basi wakatuma watu wamwite, na Yeroboamu na Israeli wote wakaja, wakamwambia Rehoboamu,
wakisema:[n] **4** "Baba yako alifanya nira yetu kuwa ngumu;[o]
na sasa wewe ufanye ule utumishi mgumu wa baba yako na ile
nira nzito[p] aliyoweka juu yetu
kuwa rahisi, nasi tutakutumikia."[q]

5 Ndipo akawaambia: "Na
kupite siku tatu. Kisha mrudi kwangu." Basi watu wakaenda zao. **6** Na Mfalme Rehoboamu akaanza kushauriana[r]
na wanaume wazee waliokuwa wakimhudumia Sulemani
baba yake sikuzote alipokuwa
angali hai, akisema: "Mnatoa
shauri gani la kuwajibu watu
hawa?"[s] **7** Basi wakasema
naye, wakimwambia: "Ukiwa

SURA 9

a 1Fa 10:27
b 2Nya 20:36
Zb 72:10
Isa 23:1
Yon 1:3
c 1Fa 9:27
d 1Fa 7:51
e 1Fa 10:18
Amo 3:15
f 1Fa 10:22
g 1Fa 3:13
1Fa 10:23
Zb 89:27
Efe 3:8
h 1Fa 3:12
1Fa 4:29
Kol 2:3
i 1Fa 4:34
j 1Fa 10:24
Isa 11:10
Lu 21:15
k 1Fa 3:28
2Nya 1:12
Met 2:6
Da 1:17
l 2Nya 26:8
Ayu 42:11
m 2Sa 8:10
n Mt 6:29
o 1Fa 10:25
p Kum 17:16
q 1Fa 4:26
r 1Fa 10:26
s 1Fa 4:21
t 2Nya 1:15
u 1Nya 27:28
v 1Fa 10:27
w Kum 17:16
2Nya 1:16
x 1Fa 10:28
Isa 31:1
y 1Fa 11:41
z 2Sa 7:2
2Sa 12:1
1Fa 1:8
1Fa 1:11
1Fa 1:32
1Nya 29:29

Safu ya 2

a 1Fa 11:36
1Fa 14:2
1Fa 14:10
b 1Fa 11:29
c 2Nya 12:15
2Nya 13:22
d 2Nya 13:20
e 1Fa 11:26
f 2Sa 5:9
1Fa 2:10
2Nya 21:20
g 1Nya 3:10
2Nya 13:7
Mhu 2:19
Mt 1:7
h 1Fa 14:21

SURA 10

i 1Fa 12:1
j Mwa 12:6
Yos 20:7
Yos 24:1
Amu 9:1
k 1Fa 11:28
l 1Fa 11:40
m 1Fa 12:2
n 1Fa 12:3
o Met 29:2
Mhu 4:1
p Mhu 5:8
q 1Fa 12:4
r 2Sa 16:20
Ayu 12:12

s 1Fa 12:6.

mwema kwa watu hawa na kuwapendeza na kusema nao maneno mema,[a] wao pia watakuwa watumishi wako sikuzote.”[b]

8 Hata hivyo, akaliacha shauri[c] la wanaume wazee walilomshauri, naye akaanza kushauriana na vijana waliokua pamoja naye,[d] waliokuwa wakimhudumia.[e] **9** Naye akawaambia: “Mnatoa shauri gani[f] ili tuwajibu watu hawa ambao wamesema nami, wakiniambia, ‘Ifanye nira ambayo baba yako aliweka juu yetu iwe rahisi’?”[g] **10** Ndipo wale vijana waliokua pamoja naye wakamwambia, wakisema: “Waambie hivi watu ambao wamesema nawe, ‘Baba yako aliifanya nira yetu kuwa nzito, lakini wewe ifanye iwe rahisi juu yetu’; wewe waambie hivi,[h] ‘Kidole changu kidogo kwa hakika kitakuwa kinene kuliko kiuno cha baba yangu.[i] **11** Na sasa baba yangu aliweka juu yenu nira nzito, lakini mimi nitaizidisha nira yenu.[j] Baba yangu aliwatia ninyi adabu kwa fimbo, lakini mimi nitawatia adabu kwa mijeledi.’”[k]

12 Na Yeroboamu na watu wote wakamjia Rehoboamu siku ya tatu, kama mfalme alivyosema: “Rudini kwangu siku ya tatu.”[l] **13** Na mfalme akaanza kuwajibu kwa ukali.[m] Basi Mfalme Rehoboamu akaliacha shauri[n] la wanaume wazee,[o] **14** naye akasema nao kulingana na lile shauri la vijana,[p] akisema: “Nitaifanya nira yenu iwe nzito zaidi, nami nitaizidisha. Baba yangu aliwatia ninyi adabu kwa fimbo, lakini mimi nitawatia adabu kwa mijeledi.”[q] **15** Na mfalme hakuwasikiliza watu; kwa maana Mungu wa kweli[r] ndiye aliyeongoza mambo ili Yehova atimize neno[a] lake alilomwambia Yeroboamu mwana wa Nebati[b] kupitia Ahiya[c] Mshilo.[d]

16 Nao Israeli wote, kwa sababu mfalme hakuwasikiliza, hao watu sasa wakamjibu mfalme, wakisema: “Tuna fungu gani katika Daudi?[e] Wala hakuna urithi katika mwana wa Yese.[f] Kila mmoja aende kwa miungu yake,[g] Ee Israeli! Sasa angalia nyumba yako mwenyewe, Ee Daudi.”[h] Kwa hiyo Israeli wote wakaanza kwenda katika mahema yao.

17 Naye Rehoboamu akaendelea kutawala juu ya wana wa Israeli waliokuwa wakikaa katika majiji ya Yuda.[i]

18 Basi Mfalme Rehoboamu akamtuma Hadoramu,[j] aliyekuwa juu ya wale walioandikishwa kufanya kazi ya kulazimishwa, lakini wana wa Israeli wakampiga kwa mawe,[k] naye akafa. Naye Mfalme Rehoboamu akafaulu kupanda katika gari lake, akakimbia kwenda Yerusalemu.[l] **19** Na Waisraeli wakaendeleza maasi[m] yao juu ya nyumba ya Daudi mpaka leo hii.

11 Rehoboamu alipofika Yerusalemu,[n] mara moja akaikutanisha nyumba ya Yuda na Benyamini,[o] wanaume bora, watu hodari wa vita,[p] watu 180,000, wapigane na Israeli ili kuurudisha ufalme kwa Rehoboamu. **2** Ndipo neno la Yehova likamjia Shemaya[q] mtu wa Mungu wa kweli, na kusema: **3** “Mwambie Rehoboamu mwana wa Sulemani mfalme wa Yuda[r] na Israeli wote katika Yuda na Benyamini, ukisema, **4** ‘Yehova amesema hivi: “Msipande kwenda kupigana na ndugu zenu.[s] Mrudi kila mmoja nyumbani kwake, kwa maana jambo hili limetokea kwa

SURA 10
a Mt 12:8; Mt 15:1; Mhu 10:4; Zek 1:13
b 1Fa 12:7
c Mt 1:25; Mt 19:20; Mhu 10:3; Isa 30:1
d Mt 13:20; Isa 3:4; 2Ti 4:3
e 1Fa 12:8
f 1Fa 22:6; Mt 21:30
g 1Fa 12:9
h 1Fa 12:10
i Ayu 31:13; Zb 140:11; Mt 10:14; Mt 18:6; Mt 28:25; Mt 29:23; Mt 23:4
j 1Sa 8:18; Isa 58:6
k 1Fa 12:11
l 1Fa 12:12
m 1Sa 20:10; Mt 10:11; Mt 12:13; Mt 14:16; Mt 15:1; Efe 4:31; Efe 6:9
n Mt 19:27
o 1Fa 12:13; Ayu 12:12
p 2Nya 22:4; Mt 12:5
q Mt 11:17; Mhu 7:7
r Kum 2:30; Zb 5:10; Mt 21:1; Amo 3:6

Safu ya 2
a 1Sa 15:29; 2Sa 17:14; 2Fa 10:10; Isa 55:11
b 1Fa 12:15
c 1Fa 11:30
d 1Fa 11:29
e 1Fa 11:13
f 2Sa 20:1
g Kut 20:3; Kum 13:5; 1Fa 12:16; Mt 11:9
h 1Fa 11:32
i 1Fa 11:36; 2Nya 11:1
j 2Sa 20:24; 1Fa 4:6; 1Fa 12:18
k Hes 14:10; 2Nya 24:21
l 1Fa 12:18
m 1Sa 10:19; 2Fa 17:21

SURA 11
n 1Fa 12:21
o Mwa 49:27; Amu 20:14; 2Nya 14:8
p Zb 33:16
q 2Nya 12:15
r 1Fa 12:23
s 2Sa 2:26; Mdo 7:26

mwongozo wangu.”’”[a] Basi wakalitii neno la Yehova, wakarudi, ili wasiende kupigana na Yeroboamu.[b]

5 Na Rehoboamu akaendelea kukaa Yerusalemu, akajenga majiji yenye ngome katika Yuda. **6** Basi akajenga upya Bethlehemu[c] na Etamu[d] na Tekoa,[e] **7** na Beth-suri[f] na Soko[g] na Adulamu,[h] **8** na Gathi[i] na Maresha[j] na Zifu,[k] **9** na Adoraimu na Lakishi[l] na Azeka,[m] **10** na Sora[n] na Aiyaloni[o] na Hebroni,[p] majiji yenye ngome, yaliyokuwa katika Yuda na Benyamini. **11** Zaidi ya hayo, akaimarisha mahali penye ngome[q] na kuweka viongozi[r] ndani yake na akiba za chakula na mafuta na divai, **12** na katika majiji yote mbalimbali akaweka ngao[s] kubwa na mikuki;[t] naye akaendelea kuyaimarisha kwa kiwango kikubwa sana. Na watu wa Yuda na Benyamini wakaendelea kuwa wake.

13 Na makuhani na Walawi waliokuwa katika Israeli yote wakasimama upande wake kutoka katika maeneo yao yote. **14** Kwa maana Walawi waliviacha viwanja vyao vya malisho[u] na miliki[v] yao kisha wakaja Yuda na Yerusalemu,[w] kwa sababu Yeroboamu[x] na wanawe walikuwa wamewaondoa[y] wasiwe makuhani kwa Yehova. **15** Naye akajiwekea mwenyewe katika cheo makuhani wa mahali pa juu[z] na wa roho waovu wenye umbo la mbuzi[a] na wa wale ndama aliokuwa ametengeneza.[b] **16** Na wale waliowafuata kutoka katika makabila yote ya Israeli, ambao walikuwa wakitoa moyo wao kumtafuta Yehova Mungu wa Israeli, wakaja Yerusalemu[c] kumtolea dhabihu[d] Yehova Mungu wa mababu zao. **17** Nao wakaendelea kuutia nguvu ufalme wa Yuda[a] na kumthibitisha Rehoboamu mwana wa Sulemani kwa miaka mitatu, kwa maana walitembea katika njia ya Daudi na Sulemani kwa miaka mitatu.[b]

18 Ndipo Rehoboamu akamchukua Mahalathi binti ya Yerimothi mwana wa Daudi awe mke wake, na ya Abihaili binti ya Eliabu[c] mwana wa Yese. **19** Baada ya muda akamzalia wana, Yeushi na Shemaria na Zahamu. **20** Na baada yake akamchukua Maaka[d] mjukuu wa Absalomu.[e] Baada ya muda akamzalia Abiya[f] na Atai na Ziza na Shelomithi. **21** Na Rehoboamu alimpenda zaidi Maaka mjukuu wa Absalomu kuliko wale wake[g] zake wengine wote na masuria wake; kwa maana alikuwa amechukua wake 18, pia masuria 60, hivi kwamba akawa na wana 28 na binti 60. **22** Kwa hiyo Rehoboamu akamweka Abiya mwana wa Maaka katika cheo awe kichwa, awe kiongozi kati ya ndugu zake, kwa maana alifikiria kumfanya kuwa mfalme. **23** Hata hivyo, akatenda kwa uelewaji[h] na kuwagawanya baadhi ya wanawe wote kwenye nchi zote za Yuda na Benyamini,[i] kwenye majiji yote yenye ngome,[j] akawapa chakula kwa wingi[k] na kuwachukulia wake wengi.[l]

12 Na ikawa kwamba mara tu ufalme wa Rehoboamu ulipofanywa imara[m] na mara tu alipokuwa na nguvu, akaiacha sheria ya Yehova,[n] na pia Israeli[o] wote pamoja naye. **2** Na ikawa kwamba katika mwaka wa tano wa Mfalme Rehoboamu,[p] Shishaki[q] mfalme

SURA 11

a 1Fa 11:31
2Nya 10:15
b 1Fa 12:24
c Mwa 35:19
Mt 2:1
d 1Nya 4:3
e 2Sa 14:2
Amo 1:1
f Yos 15:58
g 2Nya 28:18
h Yos 12:15
1Sa 22:1
i 1Nya 18:1
j Yos 15:44
k 1Sa 23:14
l Yos 10:5
2Nya 32:9
m Yos 10:10
Ne 11:30
Yer 34:7
n Yos 15:33
o Yos 19:42
p Mwa 23:2
Yos 14:15
2Sa 2:1
q Isa 22:10
r 2Nya 17:19
s 2Nya 32:5
t 2Nya 26:14
u Hes 35:3
Yos 21:21
v Hes 35:2
w Kut 32:26
Kum 33:8
x 1Fa 12:31
y Kum 12:19
z 1Fa 13:33
a Law 17:7
Isa 13:21
b 1Fa 12:28
c 2Nya 15:9
2Nya 30:11
d Kum 12:11
1Nya 22:1

Safu ya 2

a 2Nya 12:1
b 2Nya 1:1
2Nya 7:17
2Nya 8:13
Ho 6:4
c 1Sa 16:6
1Sa 17:13
d 1Fa 15:2
2Nya 11:21
e 2Sa 13:1
2Sa 18:33
f 1Fa 15:1
2Nya 12:16
Mt 1:7
g Kum 17:17
Amu 8:30
1Fa 11:3
h Met 16:20
i Yos 18:11
j 2Nya 11:11
k 2Nya 21:3
l Kum 17:17

SURA 12

m 2Nya 11:17
n Kum 8:14
Kum 32:15
2Nya 26:16
Met 30:9
o Mhu 9:18
Mik 6:16
p 1Fa 14:21
q 1Fa 11:40
1Fa 14:25

wa Misri akaja kushambulia Yerusalemu, (kwa maana walikuwa wamejiendesha kwa ukosefu wa uaminifu kwa Yehova,)[a]
3 akiwa na magari[b] 1,200 na wapanda-farasi 60,000; na hawakuwa na hesabu[c] wale watu waliotoka Misri pamoja naye —Walibya,[d] Wasukii na Waethiopia.[e] **4** Naye akayateka majiji yenye ngome yaliyokuwa ya Yuda,[f] na mwishowe akaja mpaka Yerusalemu.[g]

5 Sasa Shemaya[h] nabii akamjia Rehoboamu na wakuu wa Yuda waliokuwa wamekusanyika Yerusalemu kwa sababu ya Shishaki, naye akawaambia: "Yehova amesema hivi, 'Ninyi mmeniacha mimi,[i] nami pia nimewaacha ninyi[j] mkononi mwa Shishaki.'" **6** Ndipo wakuu wa Israeli na mfalme wakajinyenyekeza[k] na kusema: "Yehova ni mwadilifu."[l] **7** Na Yehova alipoona[m] kwamba wamejinyenyekeza, neno la Yehova likamjia Shemaya,[n] na kusema: "Wamejinyenyekeza.[o] Sitawaharibu, na baada ya kitambo kidogo nitawafanya waponyoke, na ghadhabu yangu haitamwagika juu ya Yerusalemu kwa mkono wa Shishaki.[p] **8** Lakini wao watakuwa watumishi wake,[q] ili wajue tofauti kati ya utumishi[r] wangu na utumishi kwa falme za nchi."[s]

9 Basi Shishaki[t] mfalme wa Misri akapanda kushambulia Yerusalemu, akachukua hazina za nyumba ya Yehova[u] na hazina za nyumba ya mfalme.[v] Akachukua kila kitu; kwa hiyo akazichukua zile ngao za dhahabu ambazo Sulemani alikuwa ametengeneza.[w] **10** Basi Mfalme Rehoboamu akatengeneza ngao za shaba mahali pake, akaziweka chini ya wakuu wa wakimbiaji,[a] walinzi[b] wa mlango wa nyumba ya mfalme.[c] **11** Na ikawa ikitukia kwamba kila mara mfalme akija katika nyumba ya Yehova, wakimbiaji waliingia na kuzichukua na kuzirudisha katika chumba cha walinzi cha wakimbiaji.[d] **12** Na kwa sababu alijinyenyekeza, hasira ya Yehova ikageuka,[e] ikaondoka juu yake, naye hakufikiria kuwaharibu kabisa.[f] Na zaidi ya hayo, kulikuwa na mambo mema katika Yuda.[g]

13 Na Mfalme Rehoboamu akaendelea kuimarisha cheo chake katika Yerusalemu na kuendelea kutawala; kwa maana Rehoboamu[h] alikuwa na umri wa miaka 41 alipoanza kutawala, naye akatawala miaka 17 katika Yerusalemu, jiji[i] ambalo Yehova alichagua kutoka katika makabila yote ya Israeli ili kuweka jina lake humo.[j] Na jina la mama yake lilikuwa Naama[k] Mwamoni.[l] **14** Lakini yeye alifanya yaliyokuwa mabaya,[m] kwa maana hakuwa ameufanya imara moyo wake ili kumtafuta Yehova.[n]

15 Na mambo ya Rehoboamu, ya kwanza na ya mwisho,[o] je, hayakuandikwa kati ya maneno ya Shemaya[p] nabii na Ido[q] mwonaji kulingana na maandikisho ya kiukoo? Na kulikuwa na vita kati ya Rehoboamu[r] na Yeroboamu[s] wakati wote. **16** Mwishowe Rehoboamu akalala pamoja na mababu zake,[t] akazikwa katika Jiji la Daudi;[u] na Abiya[v] mwana wake akaanza kutawala mahali pake.

13 Abiya alianza kutawala Yuda[w] katika mwaka wa kumi na nane wa Mfalme Yeroboamu. **2** Akatawala miaka mitatu katika Yerusalemu, na jina la mama yake lilikuwa

SURA 12

a Amu 2:14
2Nya 7:19
b Kut 14:9
1Fa 10:29
c Amu 6:5
d Nah 3:9
e 2Nya 14:9
2Nya 16:8
f 2Nya 11:5
Isa 36:1
g 2Fa 18:17
h 1Fa 12:22
2Nya 11:2
i Kum 28:15
2Nya 15:2
j Ayu 34:11
Ebr 10:38
k 1Fa 8:38
2Nya 33:12
2Nya 34:27
Yak 4:10
l Kut 9:27
Zb 89:14
Yer 50:7
m 1Fa 21:29
1Pe 5:5
n 1Fa 12:22
o Law 26:41
Amo 7:6
p 2Nya 12:2
q Isa 26:13
r Kum 28:47
s Ho 2:7
Ho 8:10
t 1Fa 14:25
u 1Fa 7:51
v 1Fa 14:26
2Fa 14:14
w 1Fa 10:17

Safu ya 2

a 1Sa 22:17
b 2Sa 23:23
c 1Fa 14:27
d 1Fa 14:28
e 2Nya 33:12
Isa 37:15
f Omb 3:22
g Mwa 18:24
1Fa 14:13
2Nya 19:3
h 1Fa 14:21
i Kum 12:5
2Nya 6:6
Zb 48:2
Zb 78:68
j Kut 20:24
Kum 12:11
k 1Fa 14:21
l Kum 23:3
1Fa 11:1
Ne 13:26
m 1Fa 15:34
n Kum 5:29
1Sa 7:3
1Fa 18:21
Mk 12:30
Ro 12:9
Yak 5:8
o 1Nya 29:29
p 1Fa 12:22
2Nya 11:2
q 2Nya 9:29
2Nya 13:22
r 1Fa 14:30
s 1Fa 12:20
t 1Fa 14:31
u 2Sa 5:9
v Mt 1:7

SURA 13

w 1Fa 15:1

Mikaya[a] binti ya Urieli wa Gibea.[b] Na vita vikatokea kati ya Abiya na Yeroboamu.[c]

3 Basi Abiya akaingia vitani na jeshi la wanaume wenye nguvu wa vita,[d] mia nne elfu, wanaume waliochaguliwa. Naye Yeroboamu akajipanga kivita kupigana naye akiwa na wanaume waliochaguliwa mia nane elfu, mashujaa, wanaume wenye nguvu.[e] **4** Sasa Abiya akasimama juu ya Mlima Semaraimu, ulio katika eneo lenye milima la Efraimu,[f] na kusema: "Mnisikilize, Ee Yeroboamu na Israeli wote. **5** Je, si juu yenu kujua kwamba Yehova Mungu wa Israeli mwenyewe alimpa Daudi[g] ufalme juu ya Israeli mpaka wakati usio na kipimo,[h] kwake na kwa wanawe,[i] kwa agano la chumvi?[j] **6** Na Yeroboamu[k] mwana wa Nebati, mtumishi[l] wa Sulemani mwana wa Daudi, akasimama na kumwasi[m] bwana wake.[n] **7** Na watu wazembe,[o] watu wasiofaa kitu,[p] wakaendelea kujikusanya kando yake. Mwishowe wakawa na nguvu kuliko Rehoboamu mwana wa Sulemani, wakati Rehoboamu[q] alipokuwa mchanga na mwenye moyo mwoga,[r] naye hakuweza kusimama kupigana nao.

8 "Na sasa ninyi mnafikiri juu ya kusimama imara kupigana na ufalme wa Yehova mkononi mwa wana wa Daudi,[s] huku mkiwa umati mkubwa[t] nanyi mna ndama wa dhahabu ambao Yeroboamu aliwatengenezea ninyi kuwa miungu.[u] **9** Je, hamkuwafukuza makuhani[v] wa Yehova, wana wa Haruni, na Walawi, na je, hamwendelei kujifanyia makuhani kama vikundi vya watu wa nchi?[a] Na yeyote aliyekuja na kujaza mkono wake nguvu kupitia ng'ombe-dume mchanga na kondoo-dume saba, akawa kuhani wa vitu ambavyo si miungu.[b] **10** Lakini sisi, Yehova ndiye Mungu wetu,[c] nasi hatujamwacha; lakini makuhani wanamtumikia Yehova, wana wa Haruni, na pia Walawi katika kazi.[d] **11** Nao wanamfukizia Yehova toleo la kuteketezwa asubuhi baada ya asubuhi na jioni baada ya jioni[e] na pia uvumba uliotiwa manukato;[f] na tabaka za mkate ziko juu ya meza ya dhahabu safi,[g] na kuna kinara cha taa[h] cha dhahabu na taa zake ili kuwaka jioni baada ya jioni;[i] kwa sababu tunashika wajibu[j] kwa Yehova Mungu wetu, lakini ninyi mmemwacha.[k] **12** Na tazama! pamoja nasi yuko mbele yetu Mungu wa kweli[l] pamoja na makuhani[m] wake na tarumbeta[n] za ishara kwa ajili ya kupiga king'ora cha vita juu yenu. Enyi wana wa Israeli, msipigane na Yehova Mungu wa mababu zenu,[o] kwa maana hamtafanikiwa."[p]

13 Naye Yeroboamu akapeleka kikundi cha kuvizia kizunguke kwenda nyuma yao, hivi kwamba wakawa mbele ya Yuda na kile kikundi cha kuvizia kikawa nyuma yao.[q] **14** Wakati wale wa Yuda walipogeuka, tazama, hapo walikuwa na pigano mbele na nyuma.[r] Nao wakaanza kumlilia Yehova,[s] huku makuhani wakipiga tarumbeta kwa sauti kubwa. **15** Na watu wa Yuda wakaanza kupiga kelele za vita.[t] Na ikawa kwamba, watu wa Yuda walipopiga kelele za vita, ndipo Mungu wa kweli akamshinda[u] Yeroboamu na Israeli wote mbe-

SURA 13

a 1Fa 15:2
2Nya 11:20
b Yos 18:28
1Sa 10:26
c 1Fa 15:6
d 2Nya 11:1
e Zb 33:16
f Yos 17:15
g Mwa 49:10
2Sa 7:8
Zb 78:71
h 2Sa 7:13
1Nya 17:14
i 1Nya 17:11
Zb 89:29
Lu 1:32
j Hes 18:19
Zb 89:28
k 2Nya 10:2
l 1Fa 11:26
m 1Fa 12:20
2Nya 10:18
n 1Fa 11:27
o Amu 9:4
Mdo 17:5
p Kum 13:13
1Fa 21:10
q 2Nya 10:16
r Kum 20:8
s 2Nya 9:8
t Zb 33:16
u Kum 32:17
1Fa 12:28
2Nya 11:15
Ho 8:5
v 2Nya 11:14

Safu ya 2

a 1Fa 12:31
1Fa 12:33
1Fa 13:33
b Kum 32:17
2Fa 19:18
Mdo 19:26
c Kut 19:5
2Nya 11:16
d Hes 16:40
e Kut 29:39
f Kut 30:1
2Nya 2:4
g Kut 25:30
Law 24:6
1Nya 23:29
Mt 12:4
h Kut 25:31
Kut 27:20
2Nya 4:7
i Law 24:2
j Mwa 26:5
Hes 9:19
Kum 11:1
k Kum 28:15
Zb 73:27
l Hes 23:21
Kum 20:4
Zb 20:7
Ro 8:31
m Yos 6:4
n Hes 10:9
o Isa 45:9
Mdo 5:39
p Ayu 40:9
Isa 40:15
Ebr 10:31
q Yos 8:4
r Yos 8:20
s 2Nya 14:11
2Nya 18:31
Zb 46:1
Zb 50:15
Zb 118:12
t Yos 6:16
Amu 7:18
u Hes 32:4
2Nya 14:12

le ya Abiya[a] na Yuda. **16** Na wana wa Israeli wakaanza kukimbia kutoka mbele ya Yuda, ndipo Mungu akawatia mkononi mwao.[b] **17** Na Abiya na watu wake wakawapiga kwa mauaji makubwa; na waliouawa wa Israeli wakaendelea kuanguka chini, wanaume waliochaguliwa, mia tano elfu. **18** Basi wana wa Israeli wakatiishwa wakati huo, lakini wana wa Yuda walishinda kwa sababu walimtegemea[c] Yehova Mungu wa mababu zao. **19** Na Abiya akaendelea kumfuatilia Yeroboamu, akateka majiji kutoka kwake, Betheli[d] na miji yake ya kandokando, na Yeshana na miji yake ya kandokando, na Efraini na miji yake ya kandokando.[e] **20** Na Yeroboamu hakuwa na nguvu[f] tena katika siku za Abiya; lakini Yehova akampiga,[g] hivi kwamba akafa.

21 Na Abiya akaendelea kujitia nguvu.[h] Baada ya muda akajichukulia wake 14,[i] akazaa wana 22[j] na binti 16. **22** Na yale mambo mengine ya Abiya, njia zake na maneno yake, yameandikwa katika ufafanuzi wa nabii Ido.[k]

14 Mwishowe Abiya akalala pamoja na mababu zake,[l] nao wakamzika katika Jiji la Daudi;[m] na Asa[n] mwana wake akaanza kutawala mahali pake. Katika siku zake nchi haikuwa na usumbufu[o] kwa miaka kumi.

2 Na Asa akafanya yaliyokuwa mema na sawa machoni pa Yehova Mungu wake. **3** Basi akaondoa madhabahu za kigeni[p] na mahali pa juu,[q] akazivunja nguzo takatifu[r] na kuikata miti mitakatifu.[s] **4** Tena akawaambia Yuda wamtafute[t] Yehova Mungu wa mababu zao na kutenda sheria[a] na amri.[b] **5** Kwa hiyo akaondoa katika majiji yote ya Yuda mahali pa juu na vinara vya uvumba;[c] na ufalme ukaendelea bila usumbufu[d] mbele yake. **6** Naye akajenga majiji yenye ngome katika Yuda,[e] kwa maana nchi haikuwa na usumbufu; na hapakuwa na vita juu yake wakati wa miaka hiyo, kwa maana Yehova alimpa pumziko.[f] **7** Basi akawaambia Yuda: "Acheni tujenge majiji haya na tujenge kuta[g] za kuzunguka na minara,[h] milango yenye pande mbili na mapingo.[i] Nchi bado inapatikana kwa ajili yetu, kwa sababu tumemtafuta Yehova Mungu wetu.[j] Tumemtafuta, naye anatupa pumziko kuzunguka pande zote."[k] Nao wakajenga na kufanikiwa.[l]

8 Na Asa akawa na jeshi lenye kuchukua ngao kubwa[m] na mkuki,[n] watu 300,000 kutoka Yuda.[o] Na kutoka Benyamini wale wanaochukua ngao ndogo na kupinda upinde[p] walikuwa 280,000.[q] Hao wote walikuwa mashujaa, wanaume wenye nguvu.

9 Baadaye Zera Mwethiopia[r] akaenda kupigana nao akiwa na jeshi la watu milioni moja[s] na magari mia tatu, akaja mpaka Maresha.[t] **10** Ndipo Asa akatoka kwenda juu yake, nao wakajipanga kivita katika bonde la Sefatha kule Maresha. **11** Naye Asa akaanza kumwita Yehova Mungu[u] wake, na kusema: "Ee Yehova, kwa habari ya kusaidia, si kitu kwako kama kuna wengi au wale wasio na nguvu.[v] Utusaidie, Ee Yehova Mungu wetu, kwa maana

SURA 13

a 2Nya 13:1
b Amu 1:4
c 2Fa 18:5
1Nya 5:20
2Nya 16:8
Zb 22:5
Zb 37:5
Zb 146:5
Nah 1:7
1Ti 4:10
d Yos 12:9
Amu 21:19
1Sa 13:2
1Fa 12:29
e Yoh 11:54
f Zb 18:38
g 1Sa 25:38
2Sa 12:15
1Fa 14:20
Mdo 12:23
h 2Sa 5:12
i Kum 17:17
2Sa 5:13
1Fa 11:3
j Zb 127:5
k 2Nya 9:29
2Nya 12:15

SURA 14

l Zb 49:9
Ro 5:14
m 2Sa 5:9
1Fa 2:10
1Fa 14:31
n 1Nya 3:10
o 2Nya 20:30
Met 29:2
p Kum 7:5
q Law 26:30
1Fa 11:7
1Fa 14:23
r Kut 23:24
Hes 33:52
2Fa 23:14
s Amu 6:25
2Fa 18:4
2Fa 23:6
t 2Nya 30:19
Isa 55:6
Amo 5:4
Sef 2:3
Mt 7:7

Safu ya 2

a Ne 10:29
b Zb 119:10
c 2Nya 34:4
d 2Fa 11:20
e 2Nya 8:2
2Nya 11:5
f Yos 23:1
2Nya 15:15
Zb 46:9
Met 16:7
g 2Nya 11:5
h 2Nya 32:5
i Kum 3:5
Amu 16:3
1Sa 23:7
j 1Nya 16:11
Zb 105:3
k 1Fa 5:4
l Zb 127:1
Mal 3:10
Mdo 9:31
m 1Sa 17:41
n 2Nya 11:12
o 2Nya 11:1
2Nya 13:3
p 2Nya 26:14
q Zb 68:27
Isa 60:22
r 2Fa 19:9
Mdo 8:27

s 2Nya 16:8; t Yos 15:44; Mik 1:15; u Kut 14:10; 1Nya 5:20; 2Nya 32:20; Zb 22:5; Flp 4:6; v Amu 7:7; 1Sa 14:6; Amo 5:9; 1Ko 1:27; 2Ko 12:9.

sisi tunakuegemea wewe,[a] nasi
kwa jina lako[b] tumekuja kupi-
gana na umati huu. Ee Yehova,
wewe ni Mungu wetu.[c] Usiache
mwanadamu anayeweza kufa
apate nguvu juu yako."[d]
12 Ndipo Yehova akawashin-
da[e] Waethiopia mbele ya Asa
na mbele ya Yuda, na Wae-
thiopia wakakimbia. **13** Na
Asa na watu waliokuwa pamo-
ja naye wakaendelea kuwafua-
tilia mpaka Gerari,[f] na walio
wa Waethiopia wakaendelea
kuanguka mpaka wakati amba-
po hapakuwa na yeyote aliye
hai kati yao; kwa maana wa-
livunjwa vipande-vipande mbe-
le za Yehova[g] na mbele ya je-
shi lake.[h] Baadaye wakachukua
kiasi kikubwa sana cha nyara.[i]
14 Tena wakayapiga majiji yote
pande zote kuzunguka Gerari,
kwa maana hofu[j] ya Yehova ili-
kuwa imekuja juu yao; nao wa-
kayapora majiji yote, kwa ma-
ana kulikuwa na vitu vingi
vya kupora katika majiji hayo.[k]
15 Na hata wakayapiga mahe-
ma[l] yenye mifugo hivi kwamba
wakateka[m] kwa wingi sana mi-
fugo na ngamia,[n] kisha wakaru-
di Yerusalemu.

15 Sasa roho[o] ya Mungu ika-
ja juu ya Azaria mwana
wa Odedi.[p] **2** Kwa hiyo akaen-
da mbele ya Asa na kumwa-
mbia: "Mnisikilize mimi, Ee Asa
na Yuda wote na Benyamini! Ye-
hova yuko pamoja nanyi ikiwa
ninyi mko pamoja naye;[q] nanyi
mkimtafuta,[r] atawaruhusu mu-
mpate, lakini mkimwacha yeye
atawaacha ninyi.[s] **3** Na kwa
siku nyingi Israeli[t] hawakuwa
na Mungu wa kweli wala ku-
hani mwenye kufundisha[u] wala
Sheria. **4** Lakini waliporudi
kwa Yehova Mungu wa Israe-
li,[v] wakiwa katika taabu yao,[w]

SURA 14
a 2Nya 32:8
Zb 37:5
Zb 55:22
b 1Sa 17:45
2Nya 13:12
Zb 20:5
Met 18:10
c Kum 32:3
Mk 12:29
d Yos 7:9
1Sa 2:9
Zb 9:19
Mt 6:9
e Kum 28:7
f Mwa 20:1
g Zb 68:21
h 1Nya 12:22
i 1Nya 20:2
Met 13:22
j Mwa 35:5
Kut 15:16
Kum 11:25
Yos 5:1
2Nya 17:10
k 2Nya 20:25
Zb 68:12
l 1Nya 4:41
m Hes 31:9
Hes 31:30
n 1Nya 5:21

SURA 15
o Hes 24:2
2Sa 23:2
p 2Nya 15:8
q Mal 3:7
Yak 4:8
r Isa 55:6
Yer 29:13
s 1Nya 28:9
2Nya 24:20
Ebr 10:38
t 1Fa 12:28
u Kum 33:10
2Nya 17:9
Ne 8:9
Mal 2:7
v Amu 10:10
Ho 6:1
w Kum 4:30
Zb 106:44
Ro 2:9

Safu ya 2
a Isa 55:7
Mt 7:7
b Amu 5:6
c 1Sa 13:6
d Amu 9:23
2Nya 12:15
e Kum 28:48
Amu 2:14
Zb 106:41
Ho 9:3
f Yos 1:9
1Nya 28:20
g Mhu 10:18
Ebr 12:12
h Ru 2:12
Kol 3:24
Ebr 11:6
i 2Nya 15:1
j Kum 27:15
2Fa 23:24
k Yos 17:15
l 2Nya 8:12
m 2Nya 11:16
n 2Nya 30:25
o Mwa 39:3
1Sa 18:28
Zek 8:23
Mdo 7:9

na kumtafuta, basi aliwaru-
husu wampate.[a] **5** Na nyakati
hizo hapakuwa na amani kwa
yule anayetoka wala kwa yule
anayeingia,[b] kwa sababu kuli-
kuwa na machafuko mengi kati
ya wakaaji wote wa nchi mba-
limbali.[c] **6** Nao walivunjwa
vipande-vipande, taifa kupi-
gana na taifa[d] na jiji kupigana
na jiji, kwa sababu Mungu ali-
endelea kuwatia katika macha-
fuko kwa kila namna ya taabu.[e]
7 Nanyi iweni hodari[f] na msi-
ache mikono yenu ilegee,[g] kwa
sababu kuna thawabu kwa ajili
ya kazi yenu."[h]
8 Na mara tu Asa alipoyasi-
kia maneno hayo na unabii wa
Odedi[i] nabii, akajipa moyo, aka-
ondoa kabisa machukizo[j] katika
nchi yote ya Yuda na Benyamini
na katika majiji aliyokuwa ame-
teka kutoka katika eneo lenye
milima la Efraimu,[k] na kuifa-
nya upya madhabahu ya Yehova
iliyokuwa mbele ya ukumbi wa
Yehova.[l] **9** Naye akaanza ku-
kusanya pamoja Yuda wote na
Benyamini[m] na wakaaji wage-
ni[n] waliokuwa pamoja nao ku-
toka katika Efraimu na Manase
na Simeoni, kwa maana walikuwa
wamekimbia wakamwendea
kutoka katika Israeli wakiwa
hesabu kubwa walipoona kwa-
mba Yehova Mungu wake aliku-
wa pamoja naye.[o] **10** Basi wa-
kakusanywa pamoja katika Ye-
rusalemu mwezi wa tatu wa
mwaka wa kumi na tano wa
utawala wa Asa. **11** Ndipo wa-
kamtolea Yehova dhabihu siku
hiyo kutokana na zile nyara wa-
lizoleta, ng'ombe mia saba na
kondoo elfu saba. **12** Zaidi ya
hayo, wakaingia katika agano[p]
ili kumtafuta Yehova Mungu

p 2Fa 23:3; 2Nya 34:31; Ne 10:29.

wa mababu zao kwa moyo wao
wote na kwa nafsi yao yote;[a]
13 kwamba yeyote ambaye ha-
ngemtafuta Yehova Mungu wa
Israeli, auawe,[b] iwe ni mdogo au
ni mkubwa,[c] iwe ni mwanamu-
me au ni mwanamke.[d] **14** Basi
wakamwapia[e] Yehova kwa sauti
kubwa na kwa sauti za shangwe
na kwa tarumbeta na kwa ba-
ragumu. **15** Na Yuda wote wa-
kaanza kushangilia[f] juu ya lile
jambo waliloapa; kwa maana
walikuwa wameapa kwa moyo
wao wote nao walikuwa wa-
memtafuta kwa furaha kamili
hivi kwamba yeye aliwaruhusu
wampate;[g] na Yehova akaende-
lea kuwapa pumziko kuzungu-
ka pande zote.[h]

16 Naye Asa mfalme[i] aka-
mwondoa hata Maaka[j] nyanya
yake asiwe malkia,[k] kwa sababu
alikuwa ametengeneza sana-
mu yenye kutisha kwa ajili ya
mti mtakatifu;[l] kisha Asa akai-
kata sanamu yake yenye kutis-
ha[m] na kuiponda na kuiketete-
za kwa moto[n] katika bonde la
mto la Kidroni.[o] **17** Na maha-
li pa juu[p] hapakuondolewa kati-
ka Israeli.[q] Ila moyo wa Asa
ulikuwa mkamilifu siku zake
zote.[r] **18** Naye akaanza ku-
viingiza ndani ya nyumba ya
Mungu wa kweli vitu amba-
vyo baba yake alivifanya kuwa
vitakatifu na vitu[s] ambavyo
yeye mwenyewe alivifanya
kuwa vitakatifu, fedha na dha-
habu na vyombo.[t] **19** Wala
vita havikutokea mpaka kati-
ka mwaka wa 35 wa utawala wa
Asa.[u]

16 Katika mwaka wa 36 wa
utawala wa Asa, Baasha[v]
mfalme wa Israeli alikuja kupi-
gana na Yuda na kuanza kuje-
nga Rama,[w] ili asimruhusu mtu
yeyote kutoka nje wala kuin-
gia ndani kwa Asa mfalme wa
Yuda.[a] **2** Sasa Asa akatoa fe-
dha na dhahabu katika hazi-
na za nyumba ya Yehova[b] na
nyumba ya mfalme,[c] akazipele-
ka kwa Ben-hadadi[d] mfalme wa
Siria,[e] aliyekuwa akikaa Dama-
sko,[f] akisema: **3** "Kuna agano
kati yangu na wewe na kati ya
baba yangu na baba yako. Tazа-
ma, ninakuletea fedha na dha-
habu. Nenda, vunja agano lako
na Baasha[g] mfalme wa Israeli,
ili aondoke kwangu."[h]

4 Basi Ben-hadadi akamsiki-
liza Mfalme Asa, akatuma wa-
kuu wake wa majeshi kusha-
mbulia majiji ya Israeli, hivi
kwamba wakapiga Iyoni[i] na
Dani[j] na Abel-maimu[k] na maha-
li pote penye maghala[l] pa majiji
ya Naftali.[m] **5** Na ikawa kwa-
mba mara tu Baasha aliposikia
habari hizo, mara moja akaa-
cha kujenga Rama na kuikome-
sha kazi yake.[n] **6** Naye Asa
mfalme akawachukua Yuda
wote,[o] nao wakachukua mawe
ya Rama[p] na miti yake amba-
yo Baasha alitumia kujenga,[q]
naye kwa vitu hivyo akaanza
kujenga Geba[r] na Mispa.[s]

7 Na wakati huo Hanani[t]
mwonaji akamjia Asa mfalme
wa Yuda, kisha akamwambia:
"Kwa sababu ulimwegemea mfa-
lme wa Siria[u] wala hukumwege-
mea Yehova Mungu wako,[v] kwa
sababu hiyo jeshi la mfalme wa
Siria limeponyoka kutoka mko-
noni mwako. **8** Je, Waethio-
pia[w] na Walibya[x] hawakuwa je-
shi kubwa sana kwa wingi, kwa
magari na kwa wapanda-fara-
si;[y] na kwa sababu ulimwegemea
Yehova, je, hakuwatia mkononi

SURA 15
a Kum 4:29; Yer 29:13
b Kut 22:20; Kum 17:3
c Kum 1:17
d Met 24:23
e Mhu 5:5; Mt 5:33
f Zb 5:11; Zb 40:16
g 2Nya 15:2
h Met 16:7
i Kum 13:6; Kum 33:9; Zek 13:3
j 1Fa 15:10
k 1Fa 15:13; 2Nya 19:7
l Kut 34:17
m Kum 7:5; 1Fa 15:13
n Kut 32:20
o 2Sa 15:23
p 1Fa 14:23; 2Fa 14:4; 2Fa 23:20; Eze 6:3; Eze 16:16
q 1Fa 15:14; 1Fa 22:43
r 1Fa 8:61
s 1Fa 7:51; 1Nya 26:26
t 1Fa 15:15
u 2Nya 14:1

SURA 16
v 1Fa 15:27
w Yos 18:25; Ezr 2:26; Isa 10:29

Safu ya 2
a 1Fa 15:17
b 1Fa 7:51
c 2Fa 16:8
d 1Fa 15:18
e 1Fa 20:1; 2Fa 8:7; 2Fa 12:18
f Isa 7:8
g 1Fa 15:27
h 1Fa 15:19
i 2Fa 15:29
j Mwa 14:14; Amu 18:29; Amu 20:1
k 2Sa 20:14
l 1Fa 9:19
m Yos 19:32
n 1Fa 15:21
o 1Fa 15:22
p Yos 18:25; Ezr 2:26
q 1Fa 15:17
r Yos 18:24; 1Nya 6:60; Isa 10:29; Zek 14:10
s Yos 18:26; Amu 20:1; 1Sa 7:5; Yer 40:6
t 1Fa 16:1; 2Nya 19:2; 2Nya 20:34

u Zb 146:3; Isa 31:1; Yer 17:5; v 2Fa 18:5; Ebr 12:1; w 2Nya 14:9; x 2Nya 12:3; y 2Nya 14:9.

mwako?[a] **9** Kwa maana, kwa habari ya Yehova, macho[b] yake yanaenda huku na huku duniani[c] kote ili aonyeshe nguvu zake kwa ajili ya wale ambao moyo[d] wao ni mkamilifu kumwelekea yeye. Umetenda kwa upumbavu[e] kwa habari hii, kwa maana tangu sasa na kuendelea kutakuwa na vita juu yako."[f]

10 Hata hivyo, Asa akaudhika kwa sababu ya yule mwonaji, akamtia katika nyumba ya mikatale,[g] kwa sababu alimwonea ghadhabu juu ya jambo hilo.[h] Na Asa akaanza kuwakandamiza[i] baadhi ya watu wakati huohuo. **11** Na, tazama! mambo ya Asa, ya kwanza na ya mwisho, yameandikwa katika Kitabu[j] cha Wafalme wa Yuda na wa Israeli.

12 Na Asa, katika mwaka wa 39 wa utawala wake, akapata ugonjwa katika miguu yake mpaka akawa mgonjwa sana;[k] na hata katika ugonjwa wake hakumtafuta Yehova[l] bali waponyaji.[m] **13** Mwishowe Asa akalala pamoja na mababu zake,[n] akafa katika mwaka wa 41 wa utawala wake. **14** Kwa hiyo wakamzika katika kaburi lake lenye fahari[o] alilokuwa amejichimbia katika Jiji la Daudi;[p] nao wakamlaza katika kitanda kilichojazwa mafuta ya zeri[q] na aina mbalimbali za marhamu[r] iliyochanganywa katika marhamu ya aina ya pekee.[s] Tena wakamfanyia mfukizo wa mazishi[t] ulio mkubwa isivyo kawaida.

17 Na Yehoshafati[u] mwana wake akaanza kutawala mahali pake na kuimarisha cheo chake juu ya Israeli. **2** Naye akaweka majeshi katika majiji yote yenye ngome ya Yuda na kuweka kambi za kijeshi katika nchi ya Yuda na katika majiji ya Efraimu ambayo Asa baba yake alikuwa ameyateka.[a] **3** Na Yehova akaendelea kuwa pamoja na Yehoshafati,[b] kwa sababu alitembea katika njia za zamani za Daudi babu yake[c] wala hakutafuta Mabaali.[d] **4** Kwa kuwa alimtafuta Mungu wa baba yake,[e] naye akatembea katika amri yake,[f] wala si kulingana na matendo ya Israeli.[g] **5** Na Yehova akaendelea kuufanya imara ufalme mkononi mwake;[h] na Yuda wote wakaendelea kumpa Yehoshafati zawadi,[i] naye akawa na utajiri na utukufu mwingi.[j] **6** Na moyo wake ukawa jasiri katika njia[k] za Yehova, naye akaondoa hata mahali pa juu[l] na miti mitakatifu[m] katika Yuda.

7 Na katika mwaka wa tatu wa utawala wake akawaita wakuu wake, yaani, Ben-haili na Obadia na Zekaria na Nethaneli na Mikaya, ili wafundishe katika majiji ya Yuda, **8** na pamoja nao Walawi, Shemaya na Nethania na Zebadia na Asaheli na Shemiramothi na Yehonathani na Adoniya na Tobaya na Tob-adoniya Walawi, na pamoja nao Elishama na Yehoramu makuhani.[n] **9** Nao wakaanza kufundisha[o] katika Yuda, nao walikuwa na kitabu cha sheria ya Yehova;[p] nao wakaendelea kuzunguka katika majiji yote ya Yuda na kufundisha kati ya watu.

10 Na hofu[q] ya Yehova ikawa juu ya falme zote za nchi zilizozunguka Yuda pande zote, nao hawakupigana vita na Yehoshafati.[r] **11** Na kutoka kwa Wafilisti walikuwa wakimletea Yehoshafati zawadi[s] na pesa zikiwa ushuru.[t] Pia Waarabu[u] walikuwa wakimletea makundi,

SURA 16
a 2Nya 14:11
Zb 9:10
Zb 37:40
b Ayu 34:21
Met 5:21
Yer 16:17
Ebr 4:13
1Pe 3:12
c Zek 4:10
d 1Fa 8:61
e 1Sa 13:13
f 1Fa 15:32
g 2Nya 18:26
Mhu 8:4
h Zb 37:8
Zb 141:5
Met 29:22
Ga 5:20
i Mhu 7:7
j 1Fa 15:23
k Isa 38:1
l Kum 32:39
2Fa 20:8
Zb 103:3
m Yer 17:5
n 1Fa 15:24
o 2Nya 32:33
p 2Sa 5:7
q 2Fa 20:13
r Lu 23:56
Yoh 12:7
s Mk 16:1
Yoh 19:40
t Yer 34:5

SURA 17
u 1Fa 15:24
1Fa 22:41

Safu ya 2
a 2Nya 15:8
b Yos 1:5
1Nya 22:18
Zb 46:7
Ro 8:31
c 2Sa 8:15
1Fa 11:6
1Fa 15:3
d 1Ko 10:14
e Kum 4:29
2Nya 26:5
f Lu 1:6
g 1Fa 12:28
1Fa 13:33
h 1Fa 9:5
Zb 132:12
i 1Sa 10:27
1Fa 10:25
j 1Fa 10:27
2Nya 18:1
k Zb 18:21
Zb 119:1
Ho 14:9
Yoh 2:15
Mdo 4:31
l 1Fa 22:43
2Nya 20:33
m Kum 7:5
n Kum 33:10
Mal 2:7
o Law 10:11
Ne 8:7
p Kum 31:11
Yos 1:8
2Ti 3:16
q Mwa 35:5
Kum 11:25
r Met 16:7
s 2Nya 17:5
t 2Sa 8:2
u 2Nya 9:14

kondoo-dume elfu saba na mia
saba na mbuzi-dume elfu saba
na mia saba.[a]
12 Na Yehoshafati akaende-
lea kusonga na kuwa mkuu zai-
di;[b] naye akaendelea kuje-
nga ngome[c] na majiji ya ma-
ghala[d] katika Yuda. **13** Naye
akawa na shughuli nyingi kati-
ka majiji ya Yuda; na mashujaa
wa vita,[e] wanaume wenye ngu-
vu,[f] walikuwa katika Yerusale-
mu. **14** Na hivi vilikuwa vyeo
vyao kulingana na nyumba za
mababu zao: Wa Yuda wakuu
wa maelfu, Adna mkuu, na ma-
shujaa, wanaume wenye ngu-
vu, 300,000 walikuwa pamo-
ja naye.[g] **15** Na Yehohanani
mkuu alikuwa chini yake, na
watu 280,000 walikuwa pamo-
ja naye. **16** Na Amasia mwa-
na wa Zikri mwenye kujito-
lea[h] kwa Yehova alikuwa chi-
ni yake, na mashujaa, wanaume
wenye nguvu, 200,000 waliku-
wa pamoja naye. **17** Na kuto-
ka katika Benyamini[i] paliku-
wa na yule shujaa, mwanamu-
me mwenye nguvu Eliada, na
wanaume 200,000 wenye upi-
nde na ngao walikuwa pamoja
naye.[j] **18** Na Yehozabadi ali-
kuwa chini ya amri yake, na
wanaume 180,000 waliotayari-
shwa kwa ajili ya jeshi wali-
kuwa pamoja naye. **19** Hao
ndio waliokuwa wakimhudu-
mia mfalme zaidi ya wale
ambao mfalme aliweka katika
majiji yenye ngome[k] kotekote
katika Yuda.

18 Na Yehoshafati akawa na
utajiri na utukufu kwa
wingi;[l] lakini akafanya mapata-
no ya ndoa[m] pamoja na Ahabu.[n]
2 Basi miaka fulani baadaye
akashuka kwa Ahabu huko Sa-
maria;[o] na Ahabu akamchinjia
yeye na watu waliokuwa pa-
moja naye kondoo[a] na ng'ombe
kwa wingi. Naye akaanza ku-
mshawishi[b] wapande kupiga-
na na Ramothi-gileadi.[c] **3** Na
Ahabu mfalme wa Israeli aka-
mwambia Yehoshafati mfalme
wa Yuda: "Je, utaenda pamoja
nami kule Ramothi-gileadi?"[d]
Ndipo akamwambia: "Mimi ni
sawa na wewe, na watu wangu
ni kama watu wako na tu pamo-
ja nawe katika vita."[e]
4 Hata hivyo, Yehoshafati
akamwambia mfalme wa Isra-
eli: "Tafadhali, kwanza kabisa
uliza[f] upate neno la Yehova."
5 Kwa hiyo mfalme wa Israeli
akawakusanya manabii[g] pamo-
ja, watu mia nne, akawaambia:
"Je, twende kupiga vita juu
ya Ramothi-gileadi, au nijiepu-
she?"[h] Nao wakaanza kusema:
"Panda uende, na Mungu wa
kweli atalitia jiji hilo mkononi
mwa mfalme."
6 Lakini Yehoshafati akase-
ma: "Je, hayupo hapa tena nabii
wa Yehova?[i] Basi na tuulize ku-
pitia yeye."[j] **7** Ndipo mfalme
wa Israeli akamwambia Yeho-
shafati:[k] "Bado kuna mtu mmo-
ja[l] ambaye tunaweza kumuu-
liza Yehova kupitia yeye, laki-
ni hakika mimi ninamchukia,[m]
kwa maana katika siku zake
zote yeye hatoi unabii wa mema
kunihusu mimi, ila wa ubaya.[n]
Yeye ni Mikaya mwana wa
Imla."[o] Hata hivyo, Yehoshafati
akasema: "Mfalme asiseme ja-
mbo kama hilo."[p]
8 Basi mfalme wa Israeli
akamwita ofisa wa makao ya
mfalme[q] na kusema: "Mlete ha-
raka Mikaya mwana wa Imla."[r]
9 Sasa mfalme wa Israeli na Ye-
hoshafati mfalme wa Yuda wali-
kuwa wameketi kila mmoja
juu ya kiti chake cha ufalme,
wakiwa wamevaa mavazi ya

SURA 17
a 2Fa 3:4
b 2Nya 18:1
c 2Nya 14:6
d 1Fa 9:19
2Nya 8:4
e 1Fa 9:22
f 2Nya 26:12
g 2Nya 13:3
2Nya 14:8
h Amu 5:2
Amu 5:9
Zb 110:3
i Mwa 49:27
j 2Sa 1:21
2Nya 14:8
k 2Nya 11:12
2Nya 11:23

SURA 18
l 1Sa 2:7
2Nya 17:5
Met 10:22
m 2Ko 6:14
n 1Fa 16:28
1Fa 16:33
1Fa 21:25
2Fa 8:18
o 1Fa 22:2
2Nya 19:2

Safu ya 2
a Zb 141:4
b 1Fa 22:20
Met 27:6
c Kum 4:43
1Nya 6:80
d 1Fa 22:4
e Zb 139:21
Efe 5:11
f 2Sa 2:1
1Fa 22:5
2Nya 34:26
Met 3:5
g 1Fa 18:19
h 1Fa 22:6
i 2Fa 3:11
j 1Fa 22:7
k 1Fa 22:8
l 1Fa 18:4
1Fa 19:10
m 1Fa 18:17
1Fa 21:20
Zb 34:21
n Met 15:10
Met 27:5
Isa 30:10
Yer 38:4
o 1Fa 22:8
p Met 25:12
Mik 2:7
q 1Sa 8:15
r 1Fa 22:9

kifalme,[a] nao walikuwa wameketi katika uwanja wa kupuria
kwenye mwingilio wa lango la
Samaria; na manabii wote wali-
kuwa wakitenda kama manabii
mbele yao.[b] **10** Ndipo Sede-
kia mwana wa Kenaana aka-
jitengenezea pembe[c] za chu-
ma na kusema: "Yehova ame-
sema hivi,[d] 'Kwa kutumia hizi
utawasukuma Wasiria mpaka
uwaangamize.'"[e] **11** Na wale
manabii wengine wote walikuwa wakitoa unabii kama huo, wakisema: "Panda uende Ramothi-gileadi, upate mafanikio,[f] na Yehova hakika atalitia jiji lile mkononi mwa mfalme."[g]

12 Na yule mjumbe aliyeenda kumwita Mikaya akamwambia, akisema: "Tazama! Maneno ya manabii kwa kauli moja ni mema kwa mfalme; tafadhali, neno lako na liwe kama la mmoja wao,[h] nawe useme mema."[i] **13** Lakini Mikaya akasema: "Kama Yehova anavyoishi,[j] lile ambalo Mungu wangu atasema, hilo ndilo nitakalosema."[k] **14** Ndipo akaingia kwa mfalme, naye mfalme akamwambia: "Mikaya, je, twende kupiga vita juu ya Ramothi-gileadi, au nijiepushe?" Mara moja akasema: "Panda uende na kufanikiwa; nao watatiwa mkononi mwenu."[l] **15** Kwa hiyo mfalme akamwambia: "Ninakuapisha mara ngapi[m] kwamba usiniambie jambo lolote ila kweli katika jina la Yehova?"[n] **16** Basi akasema: "Hakika ninawaona Israeli wote wametawanyika juu ya milima, kama kondoo wasio na mchungaji.[o] Na Yehova akasema: 'Hawa hawana mabwana.[p] Kila mmoja na arudi kwa amani nyumbani kwake.'"[q]

SURA 18

a Mdo 12:21
b 1Fa 22:10
c Yer 28:10
d Eze 13:6
e 1Fa 22:11
Yer 28:2
Yer 29:21
f Yer 23:25
Mik 3:5
2Pe 2:1
g 1Fa 22:12
h Zb 10:11
Isa 30:10
Ho 7:3
i 1Fa 22:13
j Kum 32:40
k 1Fa 22:14
Yer 23:28
Yer 42:4
Mdo 20:27
l 1Fa 22:15
m 1Sa 14:24
Mt 26:63
n 1Fa 22:16
o Law 26:17
Hes 27:17
Kum 28:25
Zek 10:2
p Isa 63:11
q 1Fa 22:17

Safu ya 2

a 2Nya 18:7
b Yer 2:4
c Isa 6:1
Eze 1:26
Da 7:9
Ufu 20:11
d Ayu 1:6
Da 7:10
e 1Fa 22:19
f 1Fa 22:20
g Zb 104:4
Ebr 1:7
h 1Fa 22:21
i Ayu 12:16
j Zb 33:10
2Th 2:11
k 1Fa 22:22
l Isa 19:14
Eze 14:9
m Hes 23:19
1Fa 22:23
Eze 3:19
n 2Nya 18:10
o 1Fa 22:11
p 1Fa 22:8
2Nya 18:7
q Yer 20:2
Mk 14:65
Mdo 23:2
r 1Fa 22:24
s Isa 9:14
t 1Fa 22:25

17 Ndipo mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati: "Je, sikukuambia, 'Hatatoa unabii wa mambo mema kunihusu, ila tu mabaya'?"[a]

18 Naye akaendelea kusema: "Basi sikieni neno la Yehova:[b] Hakika ninamwona Yehova ameketi juu ya kiti chake cha ufalme[c] na jeshi[d] lote la mbinguni limesimama upande wake wa kuume na wa kushoto.[e] **19** Na Yehova akasema, 'Ni nani atakayemdanganya Ahabu mfalme wa Israeli ili apande kwenda na kuanguka huko Ramothi-gileadi?' Na kukawa na mazungumzo, huyu akisema hivi, na yule akisema vile.[f] **20** Mwishowe roho[g] fulani akaja na kusimama mbele za Yehova, akasema, 'Mimi nitamdanganya.' Ndipo Yehova akamwambia, 'Kwa njia gani?'[h] **21** Naye akasema, 'Nitaenda nami nitakuwa roho ya udanganyifu katika kinywa cha manabii wake wote.'[i] Kwa hiyo akasema, 'Utamdanganya, na tena utashinda.[j] Nenda, ukafanye hivyo.'[k] **22** Na sasa, tazama, Yehova ametia roho ya udanganyifu katika kinywa cha hawa manabii wako wote;[l] lakini Yehova mwenyewe ametangaza msiba juu yako."[m]

23 Sasa Sedekia[n] mwana wa Kenaana[o] akakaribia, akampiga Mikaya[p] kwenye shavu[q] na kusema: "Ni katika njia gani hasa roho ya Yehova ilinipita mimi ikaenda kusema na wewe?"[r] **24** Kwa hiyo Mikaya akasema: "Tazama! Utaona ni njia gani siku ile[s] utakapoingia katika chumba cha ndani kabisa ili ujifiche."[t] **25** Ndipo mfalme wa Israeli akasema: "Mchukueni Mikaya, mmrudishe kwa Amoni mkuu wa jiji na

kwa Yoashi mwana wa mfalme.[a]
26 Nanyi mseme, 'Mfalme amesema hivi: "Mtieni mtu huyu
katika kizuizi,[b] mkamlishe kwa
posho iliyopunguzwa ya mkate[c]
na maji yaliyopunguzwa mpaka
nitakaporudi kwa amani."'"[d]
27 Basi Mikaya akasema: "Ukirudi kwa amani kwa vyovyote, Yehova hakusema nami." Naye akaongezea:[e] "Sikieni, enyi watu wote."[f]

28 Na mfalme wa Israeli na Yehoshafati mfalme wa Yuda wakapanda kwenda mpaka Ramothi-gileadi.[g] **29** Sasa mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati: "Mimi nitajibadili sura[h] na kuingia vitani, lakini wewe vaa mavazi yako."[i] Kwa hiyo mfalme wa Israeli akajibadili sura, kisha wakaingia vitani.[j]
30 Naye mfalme wa Siria alikuwa amewaamuru wale wakuu wa magari yake, akisema: "Msipigane na mdogo wala na mkuu, ila na mfalme wa Israeli peke yake."[k] **31** Na ikawa kwamba mara tu wale wakuu wa magari walipomwona Yehoshafati, wakaambiana: "Ndiye mfalme wa Israeli."[l] Basi wakageuka juu yake kupigana; na Yehoshafati akaanza kulia apewe msaada,[m] na Yehova akamsaidia,[n] na Mungu akawashawishi mara moja waondoke kwake.[o]
32 Na ikawa kwamba mara tu wale wakuu wa magari walipoona kwamba yeye hakuwa mfalme wa Israeli, mara moja wakaacha kumfuata.[p]

33 Na palikuwa na mtu aliyepinda upinde bila kujua, lakini akampiga[q] mfalme wa Israeli katikati ya viungio na vazi la chuma, naye akamwambia mwendesha-gari:[r] "Geuza mkono wako, uniondoe katika kambi, kwa sababu nimeumizwa vibaya."[a] **34** Na pigano likazidi kuwa kali siku hiyo, na ikawa lazima kumweka mfalme wa Israeli akiwa amesimama katika gari akiwaelekea Wasiria mpaka jioni; na mwishowe akafa wakati wa kutua kwa jua.[b]

19 Kisha Yehoshafati mfalme wa Yuda akarudi kwa
amani[c] nyumbani kwake Yerusalemu. **2** Sasa Yehu[d] mwana wa Hanani[e] mwonaji[f] akaenda mbele yake na kumwambia Mfalme Yehoshafati: "Je, waovu wanapaswa kupewa msaada,[g] na je, unapaswa kuwapenda[h] wale wanaomchukia[i] Yehova? Kwa sababu hiyo kuna ghadhabu[j] juu yako inayotoka mbele za uso wa Yehova. **3** Hata hivyo, kuna mambo mema[k] ambayo yameonekana kwako, kwa sababu umeiondoa miti mitakatifu katika nchi[l] nawe umetayarisha moyo wako kumtafuta Mungu wa kweli."[m]

4 Na Yehoshafati akaendelea kukaa Yerusalemu; naye akaanza kutoka tena na kwenda katikati ya watu kutoka Beer-sheba[n] mpaka eneo lenye milima la Efraimu,[o] ili kuwarudisha kwa Yehova Mungu wa mababu zao.[p] **5** Naye akaweka waamuzi katika nchi yote katika majiji yote yenye ngome ya Yuda, jiji baada ya jiji.[q]
6 Naye akawaambia wale waamuzi: "Oneni mnalofanya,[r] kwa sababu hamhukumu kwa ajili ya mwanadamu bali kwa ajili ya Yehova;[s] naye yupo pamoja nanyi katika jambo la hukumu.[t] **7** Na sasa hofu[u] ya Yehova na iwe juu yenu.[v] Iweni waangalifu na mtende,[w] kwa maana hakuna ukosefu wowote wa uadilifu[x] wala ubaguzi[y] wala

SURA 18
a 1Fa 22:26
b 2Nya 16:10
Yer 20:2
Mdo 5:18
c Zb 80:5
d 1Fa 22:27
e Hes 16:29
Kum 18:22
f 1Fa 22:28
g Yos 20:8
2Nya 18:2
h 1Fa 14:5
1Fa 20:38
i 1Fa 22:10
j 1Fa 22:30
k 1Fa 22:31
Met 24:6
l 1Fa 22:32
m Kut 14:10
2Nya 13:14
Zb 50:15
n Zb 34:7
Zb 46:1
Zb 94:17
o Zb 1:6
p 1Fa 22:33
q 2Fa 9:24
r 1Fa 22:34

Safu ya 2
a 2Nya 35:23
Zb 34:21
b 1Fa 22:35
2Nya 18:22

SURA 19
c 2Nya 18:31
2Nya 18:32
d 1Fa 16:1
e 2Nya 16:7
f 1Sa 9:9
g 1Fa 21:25
h Zb 139:21
Met 1:10
Met 9:8
i 1Sa 2:30
Zb 21:8
Zb 68:1
j 2Nya 32:25
Zb 90:7
Zb 141:5
k 1Fa 14:13
2Nya 17:4
l 2Nya 17:6
m 2Nya 30:19
Ezr 7:10
n Mwa 21:33
Amu 20:1
o Yos 17:15
Amu 19:1
p 1Sa 7:3
2Nya 15:8
q Kum 16:18
r Mdo 5:35
s Kum 1:17
Zb 82:1
t Kum 1:16
Yoh 5:30
Yoh 8:16
u Ne 5:15
Ayu 31:23
Met 1:7
v Kut 18:21
w 1Ti 3:2
x Mwa 18:25
Kum 32:4
Ro 9:14
y Kum 10:17
Mdo 10:34
Ro 2:11
Efe 6:9
1Pe 1:17

kuchukua rushwa kwa upande
wa Yehova Mungu wetu."[a]
8 Na katika Yerusalemu pia
Yehoshafati akaweka baadhi
ya Walawi[b] na makuhani[c] na
baadhi ya vichwa vya nyumba
za ukoo wa upande wa baba[d]
za Israeli kwa ajili ya uamu-
zi[e] wa Yehova na kwa ajili ya
kesi[f] za wakaaji wa Yerusalemu.
9 Tena akaweka amri juu yao,
akisema: "Hivi ndivyo mna-
vyopaswa kufanya katika ku-
mwogopa[g] Yehova kwa uamini-
fu na kwa moyo kamili. **10** Na
kuhusu kila kesi itakayokuja
kwenu ya ndugu zenu wanao-
kaa katika majiji yao, inayohu-
su kumwaga damu,[h] inayohusu
sheria[i] na amri[j] na masharti[k] na
maamuzi ya hukumu,[l] lazima
mwaonye kwamba wasimkosee
Yehova ili ghadhabu[m] isije juu
yenu na juu ya ndugu zenu. Hi-
vyo ndivyo mnavyopaswa kufa-
nya ili msipate hatia. **11** Na,
tazama, yupo Amaria mkuu wa
makuhani aliye juu yenu kwa
ajili ya kila jambo la Yehova;[n]
na Zebadia mwana wa Ishmae-
li kiongozi wa nyumba ya Yuda
kwa ajili ya kila jambo la mfa-
lme; nanyi mna Walawi wakiwa
maofisa kwa ajili yenu. Iweni
na nguvu,[o] mtende, na Yehova[p]
awe pamoja na mambo yaliyo
mema."[q]

20 Na ikawa kwamba ba-
adaye wana wa Moabu[r]
na wana wa Amoni[s] na pamo-
ja nao baadhi ya Waamonimu[t]
wakaja kupigana vita na Ye-
hoshafati.[u] **2** Basi watu wa-
kaja na kumwambia Yehosha-
fati, wakisema: "Umati mku-
bwa umekuja kukushambulia
kutoka katika eneo la baha-
ri, kutoka Edomu;[v] na, tazama,
wako huko Hasason-tamari, ya-
ani, En-gedi."[w] **3** Ndipo Yeho-
shafati akaogopa,[a] akauelekeza
uso wake kumtafuta Yehova.[b]
Kwa hiyo akatangaza mfungo[c]
kwa ajili ya Yuda yote. **4** Mwi-
showe watu wa Yuda wakaku-
sanyika pamoja ili kuuliza ha-
bari kutoka kwa Yehova.[d] Wa-
kaja kutoka katika majiji yote
ya Yuda ili kutafuta shauri kwa
Yehova.[e]
5 Ndipo Yehoshafati akasi-
mama katika kutaniko la Yuda
na la Yerusalemu ndani ya nyu-
mba ya Yehova[f] mbele ya ule ua
mpya,[g] **6** naye akasema:[h]
"Ee Yehova Mungu wa ma-
babu zetu,[i] je, wewe si Mungu
mbinguni,[j] na je, wewe hutawa-
li juu ya falme zote za mataifa,[k]
na je, mkononi mwako ha-
mna nguvu na uwezo, wala
hakuna anayeweza kusimama
imara kupingana nawe?[l] **7** Je,
wewe mwenyewe, Ee Mungu
wetu,[m] hukuwafukuza wakaa-
ji wa nchi hii kutoka mbele ya
watu wako Israeli,[n] kisha ukai-
kabidhi[o] kwa uzao wa Abraha-
mu, mpendwa wako,[p] mpaka
wakati usio na kipimo? **8** Nao
wakaanza kukaa ndani yake,
nao wakakujengea patakatifu
ndani yake kwa ajili ya jina
lako,[q] wakisema, **9** 'Tukipa-
twa na msiba,[r] upanga, huku-
mu mbaya, au tauni[s] au njaa,[t]
acheni tusimame mbele ya nyu-
mba hii[u] na mbele zako (kwa
maana jina lako[v] limo katika
nyumba hii), ili tukuombe msa-
ada ili kutuondoa katika taabu
yetu, nawe usikie na kuokoa.'[w]
10 Na sasa, tazama, wana wa
Amoni,[x] na Moabu[y] na eneo le-
nye milima la Seiri,[z] ambao
hukuruhusu Israeli wawava-
mie walipokuwa wakitoka kati-
ka nchi ya Misri, bali waligeu-

SURA 19
a Kum 16:19; Isa 1:23; Mik 7:3; Tit 1:7
b 2Nya 17:8
c Kum 17:9; Kum 21:5
d 1Nya 27:1
e Kum 16:18; Kum 25:1
f Kum 1:16
g 2Sa 23:3
h Kum 17:8
i Kum 4:44
j Kum 30:11; Zb 19:7
k Kum 12:1
l Kum 4:1; Zb 147:19
m Hes 16:46
n 1Nya 26:30; Mal 2:7
o Yos 1:6
p 2Nya 15:2; Zb 18:24
q Zb 37:23; Mhu 2:26

SURA 20
r Mwa 19:37; Amu 3:14; 2Sa 8:2; Zb 83:6
s Mwa 19:38
t 2Nya 20:10
u 2Nya 19:2
v Mwa 36:8; Yos 15:1
w Yos 15:62; 2Nya 20:16; 2Nya 20:20

Safu ya 2
a Mwa 32:7
b 2Nya 19:3
c Amu 20:26; Yoe 1:14; Yoe 2:12
d Kum 4:29; Zb 34:4
e 2Sa 21:1
f 2Nya 6:12; 2Nya 7:15
g 1Fa 6:36; 2Nya 4:9
h Flp 4:6
i Kut 3:6
j Kum 4:39; Yos 2:11; 1Fa 8:23; Mt 6:9
k 1Nya 29:11; Da 4:17
l 1Nya 29:12; Zb 62:11; Isa 14:27; Isa 40:15; Da 4:35
m Mwa 17:7; Kut 6:7
n Zb 44:2
o Mwa 12:7; Ne 9:8
p Isa 41:8; Yak 2:23
q 2Nya 2:4; 2Nya 6:10
r 1Fa 8:33
s 1Fa 8:37
t 2Nya 6:28
u 2Nya 6:29
v 2Nya 6:20
w 1Fa 8:34

x 2Sa 8:12; y 2Nya 20:1; z Mwa 36:8; Hes 20:18.

kia mbali kutoka kwao wala ha-
wakuwaangamiza,[a] **11** ndiyo,
tazama, wanatupa sisi thawa-
bu[b] ya kuja kutufukuza tuondo-
ke katika miliki yako ambayo
ulitufanya tuimiliki.[c] **12** Ee
Mungu wetu, je, hutafanya hu-
kumu juu yao?[d] Kwa maana ha-
kuna nguvu ndani yetu mbele
ya umati huu mkubwa unaoku-
ja juu yetu;[e] nasi wenyewe ha-
tujui tunalopaswa kufanya,[f] la-
kini macho yetu yanakuelekea
wewe."[g]

13 Na wakati huo wote watu
wote wa Yuda walikuwa wame-
simama mbele za Yehova,[h] hata
watoto wao,[i] wake zao na wana
wao.

14 Sasa kwa habari ya Yaha-
zieli mwana wa Zekaria mwa-
na wa Benaya mwana wa Yeieli
mwana wa Matania, Mlawi, wa
wana wa Asafu,[j] roho[k] ya Yeho-
va ikaja juu yake katikati ya ku-
taniko. **15** Basi akasema: "Si-
kilizeni kwa makini, Yuda wote
nanyi wakaaji wa Yerusalemu
na Mfalme Yehoshafati! Taza-
ma, Yehova amewaambia ni-
nyi hivi, 'Msiogope[l] wala msi-
we na hofu kwa sababu ya uma-
ti huu mkubwa; kwa maana
vita si vyenu bali ni vya Mu-
ngu.[m] **16** Washukieni kesho.
Tazama, wanapanda kuja kwa
njia nyembamba ya Sisi; nanyi
hakika mtawakuta mwishoni
mwa bonde la mto mbele ya nyi-
ka ya Yerueli. **17** Hamtahita-
ji kupigana[n] katika kisa hiki. Si-
mameni mahali penu, simame-
ni tuli,[o] mkauone wokovu[p] wa
Yehova kwa ajili yenu. Ee Yuda
na Yerusalemu, msiogope wala
msiwe na hofu.[q] Kesho waende-
eni, na Yehova atakuwa pamoja
nanyi.'"[r]

18 Ndipo mara moja Yeho-
shafati akainama kifudifudi,[s]
na Yuda wote na wakaaji wa
Yerusalemu wakaanguka mbe-
le za Yehova ili kumsujudia Ye-
hova.[a] **19** Kisha Walawi[b] wa
wana wa Wakohathi[c] na wa
wana wa Wakora[d] wakasima-
ma ili kumsifu Yehova Mungu
wa Israeli, kwa sauti kubwa isi-
vyo kawaida.[e]

20 Nao wakaamka asubuhi
na mapema, wakaenda katika
nyika[f] ya Tekoa.[g] Na walipoku-
wa wakienda, Yehoshafati aka-
simama na kusema: "Nisikieni,
enyi Yuda nanyi wakaaji wa Ye-
rusalemu![h] Iweni na imani[i] ka-
tika Yehova Mungu wenu, ili
mdumu muda mrefu. Iweni na
imani katika manabii wake,[j] hi-
vyo mfanikiwe."

21 Tena akafanya shauri[k] na
watu na kuweka waimbaji[l] kwa
ajili ya Yehova na wale wanao-
toa sifa[m] katika pambo taka-
tifu[n] wakienda mbele ya wale
watu wenye silaha,[o] na kusema:
"Mpeni Yehova sifa,[p] kwa maa-
na fadhili zake zenye upendo ni
za mpaka wakati usio na kipi-
mo."[q]

22 Na wakati walipoanza ku-
paaza vigelegele vya shangwe
na sifa, Yehova akaweka watu
wa kuvizia[r] juu ya wana wa
Amoni, Moabu na eneo lenye
milima la Seiri waliokuwa waki-
ja Yuda, nao wakaanza kupiga-
na wenyewe.[s] **23** Na wana wa
Amoni na Moabu wakasimama
kushambulia wakaaji wa eneo
lenye milima la Seiri[t] ili kuwaa-
ngamiza na kuwaharibu; na
mara tu walipowamaliza waka-
aji wa Seiri, wakasaidiana ku-
angamizana wao kwa wao.[u]

24 Lakini Yuda wakaja kwe-
nye mnara wa mlinzi wa nyi-
ka.[v] Walipogeuza nyuso zao

SURA 20

a Hes 20:17
Hes 20:21
Kum 2:5
Kum 2:9
Kum 2:19
Amu 11:15
b Zb 7:4
Zb 35:12
c Amu 11:23
Zb 83:4
d Amu 11:27
1Sa 3:13
Zb 7:6
e 2Nya 14:11
f 2Fa 6:15
Yer 10:23
g Zb 25:15
Zb 62:1
h Ezr 10:1
i Kum 29:11
j 1Nya 15:19
1Nya 25:1
2Nya 35:15
k Hes 11:25
2Nya 15:1
2Nya 24:20
2Pe 1:21
l Kum 1:29
Yos 11:6
2Nya 32:7
m 2Nya 32:8
n Kut 14:14
Kut 14:25
o Isa 30:15
Omb 3:26
p Kut 14:13
Kut 15:2
1Sa 2:1
1Sa 11:13
1Nya 16:23
q Kum 31:8
Yos 10:25
r Hes 14:9
2Nya 15:2
Zb 46:7
s Mwa 24:26
Kut 4:31

Safu ya 2

a Ayu 1:20
Zb 95:6
b 1Nya 15:16
c 1Nya 23:12
d Zb 44:Uta
Zb 49:Uta
e 2Nya 5:13
Zb 60:6
Zb 81:1
f 2Nya 20:16
g 2Sa 14:2
1Nya 4:5
2Nya 11:6
Yer 6:1
h 2Nya 20:15
i Kut 19:9
Isa 7:9
Ebr 11:6
j Kut 14:31
2Nya 36:16
k 1Nya 13:1
Met 11:14
l 1Nya 15:16
2Nya 5:12
2Nya 9:11
m 2Nya 29:25
Ezr 3:10
Ne 12:27
n 1Nya 16:29
Zb 29:2
Zb 96:9
o Yos 6:9
p Zb 106:1
q Kut 34:6
Omb 3:22
r Amu 7:22
1Sa 14:20

s Isa 19:2; t Mwa 14:6; Kum 2:5; u Eze 38:21; v 2Nya 20:16.

kuelekea ule umati, tazama, pale, mizoga yao ikiwa imeanguka chini[a] bila yeyote kuponyoka. **25** Basi Yehoshafati na watu wake wakaja kupora nyara[b] walizokuwa nazo, na katika nyara hizo wakakuta kwa wingi mali na mavazi na vyombo vyenye kutamanika; nao wakaendelea kuwavua mpaka waliposhindwa kuchukua zaidi.[c] Nao wakapora nyara kwa siku tatu, kwa maana zilikuwa nyingi. **26** Na katika siku ya nne wakakutana pamoja kwenye nchi tambarare ya chini ya Baraka, kwa maana walimbariki Yehova hapo.[d] Ndiyo sababu walipaita mahali hapo jina[e] Nchi Tambarare ya Chini ya Baraka—mpaka leo hii.

27 Ndipo watu wote wa Yuda na Yerusalemu wakarudi, Yehoshafati akiwa mbele yao, ili warudi Yerusalemu kwa kushangilia, kwa kuwa Yehova alikuwa amewafanya washangilie juu ya adui zao.[f] **28** Basi wakaja Yerusalemu wakiwa na vinanda[g] na vinubi[h] na tarumbeta,[i] kwenye nyumba ya Yehova.[j] **29** Na hofu[k] ya Mungu ikawa juu ya falme zote za nchi waliposikia kwamba Yehova amepiga vita juu ya adui za Israeli.[l] **30** Kwa hiyo ufalme wa Yehoshafati haukuwa na usumbufu wowote, na Mungu wake akaendelea kumpa pumziko kuzunguka pande zote.[m]

31 Na Yehoshafati[n] akaendelea kutawala juu ya Yuda. Alipoanza kutawala alikuwa na umri wa miaka 35, naye akatawala miaka 25 katika Yerusalemu. Na jina la mama yake lilikuwa Azuba[o] binti ya Shilhi. **32** Naye akaendelea kutembea katika njia ya Asa[p] baba yake, naye hakugeuka kando kutoka katika njia hiyo, kwa kutenda yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova.[a] **33** Ila tu mahali pa juu[b] hapakuondolewa; na watu walikuwa bado hawajatayarisha moyo wao kwa ajili ya Mungu wa mababu zao.[c]

34 Na mambo mengine ya Yehoshafati, ya kwanza na ya mwisho, tazama, yameandikwa kati ya maneno ya Yehu[d] mwana wa Hanani,[e] yaliyoingizwa katika Kitabu[f] cha Wafalme wa Israeli. **35** Na baada ya hayo Yehoshafati mfalme wa Yuda akawa na ushirika na Ahazia[g] mfalme wa Israeli, aliyetenda kwa uovu.[h] **36** Kwa hiyo akamfanya kuwa mshirika pamoja naye katika ujenzi wa meli za kwenda Tarshishi[i] nao wakajenga meli kule Esion-geberi.[j] **37** Hata hivyo, Eliezeri mwana wa Dodavahu wa Maresha akatoa unabii juu ya Yehoshafati, akisema: "Kwa sababu umefanya ushirika na Ahazia,[k] hakika Yehova atazivunja kazi zako."[l] Basi zile meli zikavunjwa,[m] nazo hazikuwa na nguvu za kwenda Tarshishi.[n]

21 Mwishowe Yehoshafati akalala pamoja na mababu zake,[o] akazikwa pamoja na mababu zake[p] katika Jiji la Daudi; na Yehoramu[q] mwana wake akaanza kutawala mahali pake. **2** Naye alikuwa na ndugu, wana wa Yehoshafati, Azaria na Yehieli na Zekaria na Azaria na Mikaeli na Shefatia, hao wote walikuwa wana wa Yehoshafati mfalme wa Israeli. **3** Basi baba yao akawapa zawadi[r] nyingi za fedha na dhahabu na vitu bora pamoja na majiji yenye ngome katika Yuda;[s] lakini ufalme akampa Yehoramu,[t]

SURA 20

a Kut 14:30
1Nya 5:22
Zb 110:6
Isa 37:36
b Zb 68:12
c Kut 12:35
2Fa 7:15
Met 13:22
d Kut 15:2
2Sa 22:2
Zb 103:1
e Kut 17:15
1Sa 7:12
f 1Sa 2:1
Ne 12:43
Zb 20:5
Zb 30:1
g 2Sa 6:5
1Fa 10:12
h 1Nya 13:8
1Nya 16:5
i Hes 10:8
1Nya 15:24
2Nya 29:26
j Zb 116:19
k Mwa 35:5
2Nya 14:14
2Nya 17:10
l Kut 15:14
Kum 33:26
Yos 9:9
m Yos 23:1
2Sa 7:1
2Nya 15:15
Met 16:7
n 1Fa 22:41
o 1Fa 22:42
p 1Fa 15:11

Safu ya 2

a 2Nya 17:3
Zb 18:21
b 1Fa 15:14
1Fa 22:43
2Nya 17:6
c 1Fa 18:21
2Nya 12:14
2Nya 19:3
d 1Fa 16:1
2Nya 19:2
e 2Nya 16:7
f 2Nya 16:11
g 1Fa 22:49
1Ko 15:33
h 2Fa 1:2
2Fa 1:16
2Nya 19:2
i 1Fa 10:22
1Fa 22:48
j Hes 33:35
Kum 2:8
1Fa 9:26
k Met 13:20
l Zb 127:1
m 1Fa 22:48
n 2Nya 9:21

SURA 21

o 1Fa 22:50
p 2Nya 32:33
q 2Fa 8:16
r Mwa 25:6
s 2Nya 11:23
Met 13:22
t 2Fa 8:16

kwa maana yeye ndiye aliyekuwa mzaliwa wa kwanza.[a]

4 Wakati Yehoramu aliposimama kuwa juu ya ufalme wa baba yake, alikiimarisha cheo chake, kwa hiyo akawaua ndugu zake[b] wote kwa upanga na pia baadhi ya wakuu wa Israeli. **5** Yehoramu alikuwa na umri wa miaka 32 alipoanza kutawala, naye akatawala[c] miaka 8 katika Yerusalemu. **6** Naye akaendelea kutembea katika njia ya wafalme wa Israeli,[d] kama walivyofanya wale wa nyumba ya Ahabu; kwa maana binti ya Ahabu alikuwa amekuwa mke wake,[e] naye akaendelea kufanya yaliyokuwa mabaya machoni pa Yehova.[f] **7** Na Yehova hakutaka kuiharibu nyumba ya Daudi,[g] kwa sababu ya lile agano[h] alilokuwa amefanya pamoja na Daudi, na kama alivyokuwa amesema kwamba atampa[i] yeye na wanawe taa sikuzote.[j]

8 Katika siku zake Edomu[k] waliasi kutoka chini ya mkono wa Yuda,[l] nao wakaweka mfalme atawale juu yao.[m] **9** Basi Yehoramu pamoja na wakuu wake wakavuka na pia magari yote pamoja naye. Na ikawa kwamba aliondoka wakati wa usiku, akawapiga na kuwaua Waedomu waliokuwa wamemzunguka na pia wale wakuu wa magari. **10** Lakini Edomu wakaendelea kuasi kutoka chini ya mkono wa Yuda mpaka leo hii. Wakati huo ndipo Libna[n] wakaanza kuasi kutoka chini ya mkono wake, kwa sababu yeye alikuwa amemwacha Yehova Mungu wa mababu zake.[o] **11** Yeye pia alikuwa ametengeneza mahali pa juu[p] katika milima ya Yuda, ili awasababishe wakaaji wa Yerusalemu kufanya uasherati,[a] na ili afukuzie Yuda mbali.[b]

12 Mwishowe maandishi[c] yakaja kwake kutoka kwa Eliya[d] nabii, na kusema: "Yehova Mungu wa Daudi babu yako, amesema hivi, 'Kwa sababu hukutembea katika njia za Yehoshafati[e] baba yako wala katika njia za Asa[f] mfalme wa Yuda, **13** bali unatembea katika njia ya wafalme wa Israeli[g] na kuwafanya Yuda na wakaaji wa Yerusalemu wafanye uasherati[h] kama vile nyumba ya Ahabu ilivyofanya watu wafanye uasherati,[i] na hata umewaua ndugu zako, nyumba ya baba yako, waliokuwa bora kuliko wewe;[j] **14** tazama! Yehova analeta pigo kubwa[k] kwa watu wako[l] na kwa wana wako[m] na kwa wake zako na kwa mali zako zote. **15** Nawe utakuwa na magonjwa mengi,[n] na ugonjwa wa matumbo yako, mpaka matumbo yako yatakapotoka nje kwa sababu ya ugonjwa huo siku baada ya siku.'"[o]

16 Kwa hiyo Yehova akaamsha juu ya Yehoramu roho[p] ya Wafilisti[q] na Waarabu[r] waliokuwa kando ya Waethiopia.[s] **17** Basi wakapanda na kuingia Yuda na kuifungua kwa nguvu na kuteka mali zote zilizokuwa katika nyumba ya mfalme[t] na pia wanawe na wake zake,[u] wala hakuachiwa mwana yeyote ila Yehoahazi,[v] mwana wake aliye mdogo zaidi. **18** Na baada ya hayo yote Yehova akampiga katika matumbo yake kwa ugonjwa ambao haukuweza kuponywa.[w] **19** Na ikawa kwamba katika siku zilizofuata, kipindi cha miaka miwili kamili kilipokwisha, matumbo[x] yake yakatoka nje wakati wa ugonjwa wake, na mwishowe akafa

SURA 21

a Mwa 43:33
b Mwa 4:8
Amu 9:5
c 2Fa 8:17
d 1Fa 14:9
Ho 4:1
e 2Fa 8:18
2Nya 22:2
Ne 13:26
f 1Sa 2:30
1Fa 16:25
2Nya 29:6
g 2Sa 7:16
h 2Sa 23:5
Zb 89:28
Yer 33:21
i 2Sa 7:12
j 1Fa 11:36
2Fa 8:19
Zb 132:11
k Mwa 27:40
l 2Fa 8:20
m 1Fa 22:47
n Yos 21:13
2Fa 19:8
o Kut 3:6
Kum 32:21
1Fa 11:33
2Nya 15:2
Yer 2:13
p Kum 12:2

Safu ya 2

a 2Fa 21:11
Ufu 2:20
b Kum 4:27
c Yoh 3:13
d 2Fa 2:1
2Fa 2:11
e 2Nya 17:3
f 1Fa 15:11
2Nya 14:5
g 1Fa 16:25
1Fa 16:33
h Kut 34:15
Yer 3:8
i 2Fa 9:22
2Nya 21:11
j Kut 20:13
2Nya 21:4
k Kum 28:22
l Law 26:21
Ho 5:11
Mik 6:16
m Kut 20:5
n Kum 28:61
Mdo 12:23
o Kum 28:21
p 1Fa 11:14
2Nya 33:11
Ezr 1:1
Isa 10:5
q Yos 13:2
2Sa 8:1
r 2Nya 9:14
2Nya 17:11
s 2Fa 19:9
2Nya 12:3
2Nya 14:12
t 1Fa 14:26
u 1Sa 30:3
v 2Nya 22:6
2Nya 25:23
w Kum 28:59
2Nya 21:15
Mhu 3:17
Mdo 12:23
x 2Sa 20:10

katika magonjwa yake mabaya;
na watu wake hawakumfanyia
mfukizo kama ule mfukizo[a]
waliowafanyia mababu zake.
20 Alianza kutawala akiwa na
umri wa miaka 32, naye aka-
tawala miaka 8 katika Yerusa-
lemu. Mwishowe akaenda zake
bila kutamaniwa.[b] Basi waka-
mzika katika Jiji la Daudi,[c] laki-
ni si katika makaburi ya wafa-
lme.[d]

22 Kisha wakaaji wa Yerusa-
lemu wakamfanya Aha-
zia[e] mwana wake mdogo zai-
di kuwa mfalme mahali pake,
(kwa kuwa kikundi cha wa-
poraji kilichokuja na Waara-
bu[f] kambini kilikuwa kime-
waua wale wakubwa wote,)[g]
na Ahazia mwana wa Yehora-
mu akaanza kutawala akiwa
mfalme wa Yuda. **2** Ahazia
alikuwa na umri wa miaka 22
alipoanza kutawala,[h] naye aka-
tawala mwaka mmoja katika
Yerusalemu. Na jina la mama
yake lilikuwa Athalia[i] mjukuu
wa Omri.[j]

3 Yeye pia alitembea kati-
ka njia za nyumba ya Ahabu,[k]
kwa maana mama yake[l] aliku-
wa mshauri wake katika kute-
nda maovu. **4** Naye akaende-
lea kufanya yaliyokuwa maba-
ya machoni pa Yehova, kama
nyumba ya Ahabu, kwa maana
wao walikuwa washauri[m] wake
baada ya kifo cha baba yake,
kwa uharibifu wake. **5** Yeye
pia alitembea katika shauri
lao,[n] hivi kwamba akaenda pa-
moja na Yehoramu[o] mwana wa
Ahabu mfalme wa Israeli ku-
pigana vita na Hazaeli[p] mfa-
lme wa Siria kule Ramothi-gi-
leadi,[q] ambako wapiga-mishale
walimpiga Yehoramu.[r] **6** Kwa
hiyo akarudi Yezreeli[s] ili apone
yale majeraha waliyokuwa wa-
memtia kule Rama[a] alipopiga-
na na Hazaeli mfalme wa Siria.

Naye Azaria[b] mwana wa Ye-
horamu[c] mfalme wa Yuda aka-
shuka ili amwone Yehoramu[d]
mwana wa Ahabu kule Yezreeli,
kwa maana alikuwa mgonjwa.[e]
7 Lakini kuanguka[f] kwa Aha-
zia kulitokana na Mungu,[g] ali-
pomjia Yehoramu; naye alipo-
kuja, alienda[h] pamoja na Ye-
horamu kwa Yehu[i] mjukuu wa
Nimshi,[j] ambaye Yehova aliku-
wa amemtia mafuta[k] ili aika-
tilie mbali nyumba ya Ahabu.[l]
8 Na ikawa kwamba mara Yehu
alipoanza kubishana na nyu-
mba ya Ahabu,[m] akawakuta wa-
kuu wa Yuda na wana wa ndugu
za Ahabu, wahudumu wa Aha-
zia,[n] naye akawaua.[o] **9** Kisha
akaenda kumtafuta Ahazia, na
mwishowe wakamkamata,[p] aki-
wa amejificha Samaria,[q] nao
wakamleta kwa Yehu. Kisha
wakamuua na kumzika,[r] kwa
kuwa walisema: "Yeye ni mju-
kuu wa Yehoshafati,[s] aliyemta-
futa Yehova kwa moyo wake
wote."[t] Na hapakuwa na yeyo-
te wa nyumba ya Ahazia wa ku-
shika mamlaka ya ufalme huo.
10 Kwa habari ya Athalia[u]
mama ya Ahazia, yeye aliona
kwamba mwana wake ameku-
fa. Kwa hiyo akasimama, aka-
uangamiza uzao wote wa ki-
falme wa nyumba ya Yuda.[v]
11 Hata hivyo, Yehoshabeathi[w]
binti ya mfalme akamchukua
Yehoashi[x] mwana wa Ahazia,
akamwiba kutoka kati ya wana
wa mfalme waliopaswa kuua-
wa, akamweka yeye na mle-
zi wake wa kike katika chu-
mba cha ndani cha vitanda.
Na Yehoshabeathi binti ya Mfa-
lme Yehoramu,[y] mke wa Yeho-
yada[z] kuhani, (kwa maana aliku-
wa dada ya Ahazia,) akae-

SURA 21

a 2Nya 16:14
Yer 34:5
b Met 10:7
Met 11:10
Met 29:2
Mhu 8:10
Yer 22:18
c 1Fa 2:10
d 2Nya 24:25
2Nya 28:27

SURA 22

e 2Fa 8:24
1Nya 3:11
f 2Nya 21:16
g 2Nya 21:17
h 2Fa 8:26
i 2Fa 11:1
2Fa 11:13
j 1Fa 16:28
k 1Fa 16:33
2Fa 8:27
Mik 6:16
l 2Nya 22:12
2Nya 24:7
m 2Nya 24:18
Met 1:10
Met 12:5
Met 13:20
n Zb 1:1
o 2Fa 8:25
p 2Fa 8:15
2Fa 10:32
q 1Fa 22:3
2Nya 18:14
r 2Fa 8:28
s Yos 19:18
2Sa 4:4
2Fa 9:15

Safu ya 2

a 2Fa 8:29
b 2Fa 9:16
2Nya 22:1
c 2Fa 8:16
d 2Fa 3:1
e 1Fa 22:34
f 1Sa 2:6
g Kum 32:35
Amu 14:4
2Nya 10:15
Zb 9:16
Amo 3:6
h 2Fa 9:21
i 1Fa 19:16
2Fa 9:20
j 2Fa 9:14
k 2Fa 9:6
l 2Fa 9:7
m 2Fa 10:10
2Fa 10:11
n 2Fa 10:13
o 2Fa 10:14
p 2Fa 9:27
q 2Fa 10:17
r 2Fa 9:28
s 2Nya 17:3
Met 10:7
t 2Nya 17:4
u 2Nya 22:2
v 2Fa 11:1
w 2Fa 11:2
x 2Fa 11:21
y 2Fa 8:16
z 2Nya 23:1

ndelea kumficha kwa sababu
ya Athalia, naye hakumuua.[a]
12 Naye akaendelea kuwa pa-
moja nao katika nyumba ya
Mungu wa kweli akiwa amefi-
chwa kwa miaka sita,[b] Athalia
alipokuwa akitawala kama ma-
lkia[c] juu ya nchi.[d]

23 Na katika mwaka wa
saba Yehoyada[e] akajio-
nyesha kuwa hodari, akawa-
chukua wakuu wa mamia,[f] ya-
ani, Azaria mwana wa Yeroha-
mu, na Ishmaeli mwana wa Ye-
hohanani na Azaria mwana
wa Obedi na Maaseya mwana
wa Adaya na Elishafati mwa-
na wa Zikri, pamoja naye kati-
ka agano. **2** Kisha wakazu-
nguka Yuda yote na kuwakusa-
nya Walawi[g] kutoka katika ma-
jiji yote ya Yuda na vichwa[h]
vya nyumba za ukoo wa upande
wa baba[i] za Israeli. Basi waka-
ja Yerusalemu. **3** Ndipo kuta-
niko lote wakafanya agano[j] pa-
moja na mfalme katika nyu-
mba[k] ya Mungu wa kweli, kisha
akawaambia:

"Tazama! Mwana[l] wa mfa-
lme atatawala,[m] kama Yeho-
va alivyoahidi kuhusiana na
wana wa Daudi.[n] **4** Hivi ndi-
vyo mtakavyofanya: sehemu ya
tatu kati yenu mnaoingia siku
ya sabato,[o] ya makuhani[p] na
ya Walawi,[q] watakuwa watu-
nza-milango;[r] **5** na sehemu
ya tatu watakuwa katika nyu-
mba ya mfalme;[s] na sehemu ya
tatu watakuwa kwenye Lango
la Msingi;[t] na watu wote wa-
takuwa katika nyua[u] za nyu-
mba ya Yehova. **6** Na msimru-
husu mtu yeyote aingie katika
nyumba ya Yehova[v] ila maku-
hani na wale Walawi wanaohu-
dumu.[w] Hao ndio watakaoingia,
kwa sababu wao ni kikundi
kitakatifu,[x] na watu wote wa-

SURA 22
a 2Sa 7:13
1Fa 15:4
2Nya 21:7
Zb 33:10
b 2Fa 11:3
c Kum 17:15
d Zb 12:8
Met 29:2
Yer 12:1

SURA 23
e 2Fa 11:4
f Kut 18:25
g Kum 33:8
2Nya 8:14
h 1Nya 15:12
i 1Nya 23:11
j 2Sa 5:3
2Fa 11:17
k 1Fa 7:51
l 2Fa 11:4
m 2Fa 11:12
n 2Sa 7:12
1Fa 2:4
1Fa 9:5
2Nya 6:16
2Nya 7:18
2Nya 21:7
Zb 89:29
o 1Nya 9:25
Lu 1:8
p 1Nya 24:3
q 1Nya 23:3
r 1Nya 26:1
s 1Fa 7:1
t 2Fa 11:6
u 1Fa 7:12
v 2Fa 11:7
w 1Nya 23:28
x 1Nya 23:32

Safu ya 2
a 2Fa 11:8
b 2Fa 11:4
2Nya 23:1
c Mhu 9:17
d 2Fa 11:9
e 1Nya 24:1
1Nya 25:1
1Nya 26:1
f 2Fa 11:4
1Nya 26:26
g 2Fa 11:10
h 2Sa 8:7
i 1Nya 26:27
2Nya 5:1
j 2Fa 11:11
k 2Fa 11:2
l 2Sa 1:10
2Sa 12:30
m Kum 17:18
n 1Sa 10:1
o 1Sa 10:24
p 2Fa 11:13
q 1Fa 7:15
2Fa 23:3

tashika huo wajibu kwa Yeho-
va. **7** Na Walawi wanapaswa
kumzunguka mfalme pande
zote,[a] kila mmoja akiwa na si-
laha zake mkononi mwake; na
mtu yeyote atakayeingia ndani
ya nyumba, anapaswa kuuawa.
Nanyi mwendelee kuwa
na mfalme anapoingia ndani na
anapotoka nje."

8 Na wale Walawi na Yuda
wote wakafanya kulingana na
yote ambayo Yehoyada[b] kuhani
alikuwa ameamuru.[c] Basi kila
mmoja wao akachukua watu
wake waliokuwa wakiingia wa-
kati wa sabato pamoja na wale
waliokuwa wakitoka nje waka-
ti wa sabato,[d] kwa kuwa Yeho-
yada kuhani hakuwa ameviachisha kazi vile vikundi vya mi-
gawanyo.[e] **9** Tena Yehoyada
kuhani akawapa wale wakuu
wa mamia[f] mikuki na ngao na
ngao za mviringo[g] zilizokuwa
za Mfalme Daudi,[h] ambazo zili-
kuwa katika nyumba ya Mungu
wa kweli.[i] **10** Naye akawasi-
mamisha watu wote,[j] kila mmo-
ja akiwa na silaha yake mkono-
ni mwake, kuanzia upande wa
kuume wa nyumba mpaka upa-
nde wa kushoto wa nyumba,
kando ya madhabahu na ka-
ndo ya nyumba, pande zote ka-
ribu na mfalme. **11** Kisha wa-
kamtoa nje mwana wa mfalme,[k]
wakamvika taji[l] na ule Ushu-
huda,[m] wakamfanya kuwa mfa-
lme, hivyo Yehoyada na wanawe
wakamtia mafuta[n] na kusema:
"Mfalme na aishi!"[o]

12 Athalia aliposikia sauti
ya watu wakikimbia na kumsi-
fu mfalme,[p] mara moja akai-
ngia kwa watu katika nyumba
ya Yehova. **13** Kisha akao-
na, na tazama, mfalme aliku-
wa amesimama kando ya ngu-
zo[q] yake katika mwingilio, na

wakuu[a] na tarumbeta[b] kando ya mfalme, na watu wote wa nchi walikuwa wakishangilia[c] na kupiga[d] tarumbeta, na waimbaji[e] walikuwa na vyombo vya nyimbo na wale wanaotoa ishara za kutoa sifa. Athalia akayararua mavazi yake mara moja na kusema: "Ni hila! Ni hila!"[f] **14** Lakini Yehoyada kuhani akawatoa nje wale wakuu wa mamia, watu waliochaguliwa wa jeshi, na kuwaambia: "Mwondoeni katikati ya vikosi;[g] na yeyote atakayemfuata, auawe kwa upanga!" Kwa maana kuhani yule alikuwa amesema: "Msimuue ndani ya nyumba ya Yehova." **15** Basi wakamkamata. Alipofika katika mwingilio wa lango la farasi la nyumba ya mfalme, wakamuua hapo mara moja.[h]

16 Ndipo Yehoyada akafanya agano kati yake na watu wote na mfalme kwamba wao wataendelea kuwa watu[i] wa Yehova. **17** Kisha watu wote wakaenda kwenye nyumba ya Baali, wakaibomoa;[j] nao wakazivunja madhabahu[k] zake na sanamu[l] zake, nao, mbele ya zile madhabahu, wakamuua[m] Matani[n] kuhani wa Baali. **18** Tena Yehoyada akavitia vyeo vya nyumba ya Yehova mkononi mwa makuhani na Walawi, ambao Daudi[o] alikuwa amewaweka katika migawanyo juu ya nyumba ya Yehova ili watoe dhabihu za kuteketezwa za Yehova kulingana na yale ambayo yameandikwa katika sheria ya Musa,[p] kwa kushangilia pamoja na nyimbo kwa mikono ya Daudi. **19** Kwa hiyo akawaweka watunza-malango[q] kando ya malango[r] ya nyumba ya Yehova ili yeyote aliye najisi katika jambo lolote asiingie.

SURA 23

a 2Nya 23:1
b Hes 10:10
1Nya 15:24
c 1Fa 1:40
Met 11:10
d 1Fa 1:39
2Fa 9:13
e 1Nya 25:7
f 2Fa 11:14
g 2Fa 11:15
h 2Fa 11:16
i 2Fa 11:17
2Nya 34:31
j 2Fa 10:27
k Kum 12:3
2Nya 34:4
2Nya 34:7
l Kut 32:20
m Kum 13:5
Kum 13:9
1Fa 18:40
n 2Fa 11:18
o 1Nya 23:6
1Nya 23:30
p Kut 29:38
Hes 28:2
q 1Nya 26:1
1Nya 26:13
r 1Nya 9:26

Safu ya 2

a 2Fa 11:9
b 2Fa 11:19
c 1Fa 1:13
1Fa 7:7
d Met 11:10
Met 29:2
e 2Fa 11:20

SURA 24

f 2Fa 11:21
2Ko 3:5
g 2Fa 12:1
h Mwa 21:14
2Sa 3:10
i 1Nya 3:11
j 2Nya 26:4
k 2Fa 12:2
l Zb 127:3
m 2Fa 22:5
2Nya 34:8
n 2Fa 12:4
o 2Nya 29:3
2Nya 34:9
p 2Fa 12:5
q 2Fa 12:6
Met 10:4
Mhu 10:18
r 2Fa 12:7
s Kut 30:12
Kut 30:13
Kut 30:14
Kut 30:16
t Hes 1:50
Mdo 7:44

20 Sasa akawachukua wakuu wa mamia[a] na mabwana na watawala juu ya watu na watu wote wa nchi na kumshusha mfalme kutoka katika nyumba ya Yehova.[b] Kisha wakaja moja kwa moja kupitia lango la juu mpaka kwenye nyumba ya mfalme, wakamketisha mfalme juu ya kiti cha ufalme.[c] **21** Na watu wote wa nchi wakaendelea kushangilia;[d] nalo jiji halikuwa na usumbufu, nao walikuwa wamemuua Athalia kwa upanga.[e]

24 Yehoashi[f] alikuwa na umri wa miaka 7 alipoanza kutawala, naye akatawala miaka 40 katika Yerusalemu.[g] Na jina la mama yake lilikuwa Sibia kutoka Beer-sheba.[h] **2** Na Yehoashi[i] akaendelea kufanya yaliyokuwa sawa machoni[j] pa Yehova siku zote za Yehoyada kuhani.[k] **3** Na Yehoyada akampa wake wawili, naye akazaa wana na mabinti.[l]

4 Ikawa baadaye kwamba kurekebisha nyumba ya Yehova kukawa moyoni mwa Yehoashi.[m] **5** Kwa hiyo akawakusanya makuhani[n] na Walawi na kuwaambia: "Nendeni katika majiji ya Yuda, mkusanye pesa kutoka kwa Israeli wote ili kuirekebisha[o] nyumba ya Mungu wenu mwaka baada ya mwaka;[p] nanyi mtende jambo hili haraka." Na Walawi hawakutenda haraka.[q] **6** Basi mfalme akamwita Yehoyada aliye kichwa na kumwambia:[r] "Kwa nini hujawadai Walawi walete kutoka Yuda na Yerusalemu kodi takatifu iliyoagizwa na Musa[s] mtumishi wa Yehova, ile ya kutaniko la Israeli, kwa ajili ya hema la Ushuhuda?[t] **7** Kwa maana wana wa Athalia yule mwanamke

mwovu[a] walikuwa wamevunja
na kuingia ndani ya nyumba
ya Mungu wa kweli,[b] na hata
vitu vyote vitakatifu[c] vya nyu-
mba ya Yehova walikuwa wa-
mevitolea Mabaali."[d] **8** Ndipo
mfalme akatoa amri, nao waka-
tengeneza sanduku[e] na kuliwe-
ka nje kwenye lango la nyumba
ya Yehova. **9** Kisha wakatoa
mwito katika Yuda na Yerusa-
lemu yote ili kumletea Yeho-
va ile kodi takatifu[f] iliyoagizwa
na Musa[g] mtumishi wa Mungu
wa kweli juu ya Israeli nyikani.
10 Na wakuu[h] wote na watu
wote wakaanza kushangilia,[i]
nao wakaendelea kuleta na ku-
itia ndani ya lile sanduku[j] mpa-
ka wote walipokuwa wametoa.

11 Na ikawa kwamba kwa
wakati unaofaa akawa akiliwe-
ka lile sanduku chini ya ua-
ngalizi wa mfalme kwa mkono
wa Walawi,[k] na mara tu wali-
poona kuna pesa nyingi,[l] mwa-
ndishi[m] wa mfalme na mjumbe
wa mkuu wa makuhani waka-
ja na kuzitoa katika sandu-
ku, kisha wakaliinua na kulir-
disha mahali pake. Hivyo ndi-
vyo walivyofanya siku baada
ya siku, hivi kwamba wakaku-
sanya pesa kwa wingi. **12** Ki-
sha mfalme na Yehoyada waka-
wa wakiwapa waliokuwa waki-
fanya[n] kazi katika utumishi wa
nyumba ya Yehova,[o] nao wakaa-
ndika wachongaji wa mawe[p] na
mafundi[q] ili kuirekebisha nyu-
mba ya Yehova,[r] na pia wafa-
nyakazi wa chuma na shaba ili
kuirekebisha nyumba ya Yeho-
va.[s] **13** Na wafanyakazi wa-
kaanza kutenda,[t] na kazi ya
kurekebisha ikaendelea kuso-
nga mbele mkononi mwao,
na mwishowe wakaisimamisha
nyumba ya Mungu wa kweli
kama inavyopaswa kuwa kimu-
undo na kuitia nguvu. **14** Na
mara tu walipomaliza, wakale-
ta pesa zilizobaki mbele ya
mfalme na Yehoyada, nao waka-
tengeneza vyombo vya nyumba
ya Yehova, vyombo vya hudu-
ma[a] na vya kutoa matoleo na
vikombe[b] na vyombo vya dha-
habu[c] na vya fedha; nao waka-
wa watoaji wa dhabihu za kute-
keteza wa[d] katika nyumba ya Ye-
hova kwa ukawaida siku zote
za Yehoyada.

15 Na Yehoyada akawa mzee
na mwenye kushiba miaka[e]
naye akafa mwishowe, akiwa
na umri wa miaka 130 wakati
wa kifo chake. **16** Basi waka-
mzika katika Jiji la Daudi pa-
moja na wafalme,[f] kwa sababu
alikuwa ametenda mema kati-
ka Israeli[g] na kwa Mungu wa
kweli na kwa nyumba Yake.

17 Na baada ya kifo cha Ye-
hoyada, wakuu[h] wa Yuda waka-
ja na kumwinamia mfalme.
Na wakati huo mfalme aka-
wasikiliza.[i] **18** Na mwishowe
wakaiacha nyumba ya Yehova
Mungu wa mababu zao, waka-
anza kuitumikia miti mitakati-
fu[j] na sanamu,[k] hivi kwamba
kukawa na ghadhabu juu ya
Yuda na Yerusalemu kwa saba-
bu ya hiyo hatia yao.[l] **19** Naye
akaendelea kutuma manabii[m]
katikati yao ili kuwarudisha
kwa Yehova; nao wakaendelea
kutoa ushuhuda juu yao, laki-
ni hawakusikiliza.[n]

20 Na roho[o] ya Mungu ika-
mfunika[p] Zekaria[q] mwana wa
Yehoyada[r] kuhani, hivi kwamba
akasimama juu ya watu na ku-
waambia: "Mungu wa kweli
amesema hivi, 'Kwa nini mnazi-
vunja amri za Yehova, hivi kwa-
mba hamwezi kufanikiwa?[s] Kwa
sababu mmemwacha Yehova,
yeye naye atawaacha ninyi.'"[t]

SURA 24

a 2Nya 22:3
b 2Nya 28:24
c 2Fa 12:4
2Fa 14:14
d Kum 32:17
Eze 16:17
Ho 2:13
e 2Fa 12:9
Mk 12:41
f Ne 10:32
Mt 17:24
g Kut 30:12
Kut 30:13
Kut 30:14
Kut 30:16
h 1Nya 28:1
i 1Nya 29:9
Isa 64:5
Mdo 2:46
j 2Fa 22:9
k 2Nya 34:9
l 2Fa 22:9
m 2Fa 12:10
n 1Ti 5:18
o 2Fa 12:11
p 1Fa 5:17
q 2Nya 34:11
r 2Fa 12:12
s 2Nya 34:8
t 2Nya 34:12

Safu ya 2

a 1Fa 7:50
b Kut 37:16
Hes 7:84
c 2Nya 4:21
2Nya 4:22
d Kut 29:28
Hes 28:3
e Zb 91:16
f 1Fa 2:10
2Nya 24:25
Mdo 2:29
g 2Nya 23:1
Met 10:7
Ebr 6:10
h 1Nya 28:1
i Met 11:9
Met 29:12
j 1Fa 14:23
k 1Fa 14:9
l Ne 9:26
Zb 102:10
m 2Fa 17:13
Yer 7:25
n 2Nya 36:16
o Hes 11:25
2Nya 15:1
2Nya 20:14
2Pe 1:21
p Amu 6:34
1Nya 12:18
q Lu 11:51
r 2Nya 23:11
s Hes 14:41
1Sa 13:13
Zek 7:11
t Kum 29:25
1Nya 28:9
2Nya 15:2
Yer 2:19

21 Mwishowe wakapanga hila
juu yake,[a] wakampiga kwa
mawe[b] kwa amri ya mfalme ka-
tika ua wa nyumba ya Yehova.
22 Na Yehoashi mfalme haku-
kumbuka fadhili zenye upendo
ambazo Yehoyada baba yake
alikuwa amemwonyesha,[c] hivi
kwamba akamuua mwana wake,
ambaye, alipokuwa akifa, alise-
ma: "Yehova na aone jambo hili
na kulidai."[d]

23 Na ikawa kwamba mwa-
nzoni mwa mwaka,[e] jeshi la
Siria[f] likaja kupigana naye,[g]
nao wakaanza kuvamia Yuda
na Yerusalemu. Ndipo waka-
waangamiza wakuu[h] wote wa
watu kutoka katikati ya watu,
nao wakapeleka nyara yao
yote kwa mfalme wa Damasko.[i]
24 Kwa maana jeshi la Wasi-
ria lilivamia kwa hesabu ndogo
ya watu,[j] na Yehova mwenyewe
akatia mkononi mwao jeshi lili-
lo na hesabu kubwa sana,[k] kwa
sababu walikuwa wamemwa-
cha Yehova Mungu wa maba-
bu zao; nao wakafanya hukumu
juu ya Yehoashi.[l] **25** Nao wali-
poondoka kwake (kwa kuwa
walimwacha akiwa na magon-
jwa mengi),[m] watumishi wake
mwenyewe wakapanga hila[n]
juu yake kwa sababu ya damu[o]
ya wana wa Yehoyada[p] kuha-
ni; wakamuua kitandani mwa-
ke, hata akafa.[q] Kisha waka-
mzika katika Jiji la Daudi,[r] laki-
ni hawakumzika katika maka-
buri ya wafalme.[s]

26 Na hawa ndio waliopa-
nga hila juu yake: Zabadi[t] mwa-
na wa Shimeathi mwanamke
Mwamoni na Yehozabadi mwa-
na wa Shimrithi mwanamke
Mmoabu. **27** Na kwa habari
ya wanawe na wingi wa mata-
ngazo juu yake[u] na kuwekwa
msingi[v] wa nyumba ya Mungu
wa kweli, tazama, yameandi-
kwa katika ufafanuzi wa Kita-
bu[a] cha Wafalme. Na Amazia[b]
mwana wake akaanza kutawa-
la mahali pake.

25 Amazia[c] alikuwa mfalme
akiwa na umri wa mia-
ka 25, naye akatawala mia-
ka 29 katika Yerusalemu.
Na jina la mama yake lilikuwa Yehoadani[d] wa Yerusalemu.
2 Naye akaendelea kufanya yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova,[e] ila tu si kwa moyo kamili.[f] **3** Na ikawa kwamba mara tu ufalme ulipokuwa umeimarishwa kwake, akawaua[g] mara moja wale watumishi[h] wake waliompiga na kumuua mfalme, baba yake.[i] **4** Naye hakuwaua wana wao, bali alifanya kulingana na yale ambayo yameandikwa katika sheria, katika kitabu cha Musa,[j] ambayo Yehova aliamuru, akisema: "Akina baba wasife kwa sababu ya wana,[k] wala wana wasife kwa sababu ya akina baba;[l] bali kila mmoja afe kwa sababu ya dhambi yake mwenyewe."[m]

5 Na Amazia akawakusanya Yuda na kuwasimamisha kulingana na nyumba ya mababu,[n] kulingana na wakuu wa malfu[o] na kulingana na wakuu wa mamia[p] kwa ajili ya Yuda wote na Benyamini; naye akawaandikisha kuanzia umri wa miaka 20[q] na zaidi, na mwishowe akakuta kwamba walikuwa wanaume bora 300,000 wanaoingia jeshini, wanaotumia mkuki[r] na ngao kubwa.[s] **6** Tena akaandika kutoka katika Israeli mashujaa, wanaume wenye nguvu mia moja elfu kwa talanta mia moja za fedha. **7** Na mtu fulani wa Mungu wa kweli[t] akamjia, akisema: "Ee mfalme, usiache jeshi la Israeli liende

SURA 24
a Yer 11:19; Yer 18:18
b Mt 23:35; Lu 11:51; Mdo 7:58
c Ayu 6:14; Met 17:13
d Mwa 9:5; Zb 94:1; Yer 11:20; Ebr 10:30; Yud 9
e 1Fa 20:22
f 2Fa 12:17
g Kum 32:35
h 2Nya 24:17
i Mwa 14:15; 1Nya 18:5
j Law 26:37; Kum 32:30
k Law 26:25; Kum 28:25
l 2Nya 22:8; Isa 10:5; Hab 1:12
m Kum 28:22; 2Nya 21:18
n 2Fa 14:19
o Mwa 9:5; 2Nya 24:21; Lu 11:51; Ufu 16:6
p 2Nya 24:20
q 2Sa 4:7; 2Fa 12:20
r 2Sa 5:9; 1Fa 2:10
s 2Nya 21:20; 2Nya 28:27; Zb 69:28
t 2Fa 12:21
u 2Nya 24:20
v 2Nya 24:13

Safu ya 2
a 2Fa 12:19; 2Nya 20:34
b 2Fa 12:21; 1Nya 3:12

SURA 25
c 2Fa 14:1
d 2Fa 14:2
e Kum 12:32
f 1Fa 8:61; 1Fa 11:4; 2Fa 14:3; Zb 78:37
g Mwa 9:6; Kut 21:14; Hes 35:31
h 2Nya 24:26
i 2Nya 24:25
j Kum 24:16
k Eze 18:20
l Eze 18:4
m 2Fa 14:6
n 1Nya 27:1
o Kut 18:25; 1Sa 8:12; 1Nya 13:1
p Kum 1:15
q Hes 1:3
r 1Nya 12:24; 2Nya 11:12
s 2Nya 32:5
t 1Fa 13:1

pamoja nawe, kwa maana Yehova hayuko pamoja na Israeli,[a] yaani, wana wote wa Efraimu. **8** Lakini wewe mwenyewe nenda, utende, uwe hodari kwa ajili ya vita.[b] Mungu wa kweli anaweza kukufanya ujikwae mbele ya adui; kwa maana Mungu ana nguvu za kusaidia[c] na za kusababisha kujikwaa."[d] **9** Ndipo Amazia[e] akamwambia yule mtu wa Mungu wa kweli: "Lakini zifanyweje zile talanta mia moja ambazo nimewapa majeshi ya Israeli?"[f] Mtu wa Mungu wa kweli akajibu, akasema: "Yehova ana uwezo wa kukupa nyingi zaidi kuliko hizo."[g] **10** Basi Amazia akawatenga, yaani, yale majeshi yaliyomjia kutoka Efraimu, ili waende kwao. Hata hivyo, hasira yao ikawaka sana juu ya Yuda, nao wakarudi kwao wakiwaka hasira.[h]

11 Naye Amazia akajipa moyo, akawaongoza watu wake, akaenda katika Bonde la Chumvi;[i] naye akawapiga wana wa Seiri,[j] elfu kumi kati yao.[k] **12** Na wana wa Yuda wakakamata watu elfu kumi wakiwa hai. Basi wakawaleta kwenye kilele cha mwamba, wakawatupa kutoka kilele cha mwamba ule; nao wote wakapasuka.[l] **13** Na wale askari-jeshi ambao Amazia alirudisha wasiende pamoja naye vitani,[m] wakaanza kuvamia majiji ya Yuda, kuanzia Samaria[n] mpaka Beth-horoni,[o] wakawapiga elfu tatu kati yao na kuchukua nyara nyingi.

14 Lakini ikawa kwamba baada ya Amazia kurudi kutoka kuwapiga Waedomu, akaleta miungu[p] ya wana wa Seiri na kujisimamishia iwe miungu,[q] naye akaanza kuinama mbele yake,[a] naye akaanza kuifukizia moshi wa dhabihu.[b] **15** Kwa hiyo hasira ya Yehova ikawaka juu ya Amazia, na hivyo akamtumia nabii na kumwambia: "Kwa nini umeitafuta[c] miungu ya watu[d] ambayo haikuwakomboa watu wake kutoka mkononi mwako?"[e] **16** Na ikawa kwamba aliposema naye, mara moja mfalme akamwambia: "Je, tulikuweka wewe kuwa mshauri wa mfalme?[f] Acha kwa faida yako mwenyewe.[g] Kwa nini wakupige na kukuua?" Kwa hiyo yule nabii akaacha, lakini akasema: "Hakika ninajua kwamba Mungu ameazimia kukuangamiza wewe,[h] kwa sababu umetenda hivi[i] wala hukulisikiliza shauri langu."[j]

17 Na Amazia mfalme wa Yuda akatafuta shauri na kutuma ujumbe kwa Yehoashi mwana wa Yehoahazi mwana wa Yehu mfalme wa Israeli,[k] na kusema: "Njoo! Tutazamane uso kwa uso."[l] **18** Ndipo Yehoashi mfalme wa Israeli akatuma ujumbe kwa Amazia mfalme wa Yuda, na kusema:[m] "Gugu lenye miiba lililokuwa katika Lebanoni lilituma ujumbe kwa mwerezi uliokuwa katika Lebanoni,[n] na kusema, 'Mpe mwanangu binti yako awe mke wake.'[o] Hata hivyo, mnyama wa mwituni[p] aliyekuwa katika Lebanoni akapita karibu, akalikanyaga lile gugu lenye miiba. **19** Umesema moyoni mwako, Tazama, umepiga Edomu.[q] Na moyo[r] wako umekuinua ili utukuzwe.[s] Sasa endelea kukaa nyumbani kwako mwenyewe.[t] Kwa nini ujiingize katika mzozo katika hali zisizofaa[u] hata uanguke, wewe na Yuda pamoja nawe?"[v]

SURA 25

a 2Nya 13:16
2Nya 19:2
b Met 24:10
c 2Nya 14:11
2Nya 20:6
Zb 33:20
d Yer 18:23
e 2Fa 14:1
f 2Nya 25:6
g 1Sa 2:7
Met 10:22
Hag 2:8
h 2Sa 19:43
Met 29:22
i 2Sa 8:13
Zb 60:Uta
j 2Nya 20:10
k 2Fa 14:7
l Oba 3
Mdo 1:18
m 2Nya 25:9
n 1Fa 16:24
1Fa 16:29
o 1Fa 9:17
2Nya 8:5
p 2Nya 28:23
q Kut 20:3
Kum 7:5
Kum 7:25

Safu ya 2

a Kut 20:5
b 2Nya 28:25
2Nya 34:25
c 2Nya 24:20
Yer 2:5
d Zb 96:5
e Zb 115:8
Isa 46:2
Yer 10:5
1Ko 8:4
1Ko 10:20
f 2Nya 16:10
2Nya 18:25
g Met 9:7
Met 15:10
Isa 30:10
2Ti 4:3
h Eze 18:26
i 1Sa 2:25
j Met 29:1
k 2Fa 14:8
l Met 20:3
m 2Fa 14:9
n 1Fa 4:33
o Amu 9:8
p Zb 80:13
q 2Nya 25:11
r Kum 8:14
2Nya 26:16
2Nya 32:25
Met 16:18
Met 28:25
Da 5:20
Hab 2:4
s Met 29:23
Yer 9:23
t Met 12:15
u 2Fa 14:10
v 2Nya 35:21

20 Lakini Amazia hakusikiliza; kwa maana jambo hilo lilitoka kwa Mungu wa kweli[a] kwa kusudi la kuwatia mkononi mwake, kwa sababu walikuwa wameitafuta miungu ya Edomu.[b] **21** Basi Yehoashi mfalme wa Israeli akapanda,[c] nao wakatazamana uso kwa uso,[d] yeye na Amazia mfalme wa Yuda, kule Beth-shemeshi,[e] ya Yuda. **22** Na Yuda wakashindwa mbele ya Israeli,[f] hata wakaanza kukimbia, kila mmoja kwenda katika hema lake.[g] **23** Naye Yehoashi mfalme wa Israeli akamkamata[h] Amazia mfalme wa Yuda, mwana wa Yehoashi mwana wa Yehoahazi, kule Beth-shemeshi, kisha akamleta Yerusalemu,[i] naye akabomoa shimo katika ukuta wa Yerusalemu, kuanzia Lango la Efraimu[j] mpaka kwenye Lango la Pembeni,[k] urefu wa mikono mia nne. **24** Naye akachukua dhahabu yote na fedha na vyombo vyote vilivyopatikana katika nyumba ya Mungu wa kweli na Obed-edomu[l] na hazina za nyumba ya mfalme[m] na mateka, kisha akarudi Samaria.[n]

25 Na Amazia[o] mwana wa Yehoashi mfalme wa Yuda akaendelea kuishi miaka kumi na mitano baada ya kifo cha Yehoashi mwana wa Yehoahazi mfalme wa Israeli.[p] **26** Na mambo mengine ya Amazia, ya kwanza na ya mwisho,[q] tazama! je, hayakuandikwa katika Kitabu[r] cha Wafalme wa Yuda na Israeli?[s] **27** Na kutoka wakati Amazia alipogeuka akaacha kumfuata Yehova, wakapanga hila[t] juu yake katika Yerusalemu. Mwishowe akakimbilia Lakishi;[u] lakini wakatuma watu kumfuatilia huko Lakishi, wakamuua huko.[a] **28** Kwa hiyo wakambeba juu ya farasi,[b] wakamzika pamoja na mababu zake katika jiji la Yuda.[c]

26 Ndipo watu[d] wote wa Yuda wakamchukua Uzia,[e] akiwa na umri wa miaka kumi na sita, nao wakamfanya[f] kuwa mfalme mahali pa Amazia[g] baba yake. **2** Yeye ndiye aliyejenga upya Elothi[h] kisha akalirudisha kwa Yuda baada ya mfalme kulala pamoja na mababu zake.[i] **3** Uzia[j] alianza kutawala akiwa na umri wa miaka 16, naye akatawala miaka 52 katika Yerusalemu. Na jina la mama yake lilikuwa Yekolia[k] wa Yerusalemu. **4** Naye akaendelea kufanya yaliyokuwa sawa machoni pa Yehova,[l] kulingana na yote ambayo Amazia baba yake alikuwa amefanya.[m] **5** Naye akaendelea kuwa na mwelekeo wa kumtafuta[n] Mungu katika siku za Zekaria, aliyekuwa akiwafundisha watu kumwogopa Mungu wa kweli;[o] na katika zile siku alizokuwa akimtafuta Yehova, Mungu wa kweli alimfanikisha.[p]

6 Naye akatoka kwenda kupigana na Wafilisti,[q] akapenya ukuta wa Gathi[r] na ukuta wa Yabne[s] na ukuta wa Ashdodi,[t] kisha akajenga majiji katika eneo la Ashdodi[u] na katikati ya Wafilisti. **7** Na Mungu wa kweli akaendelea kumsaidia[v] juu ya Wafilisti na juu ya Waarabu[w] waliokuwa wakikaa katika Gurbaali na Meunimu.[x] **8** Na Waamoni[y] wakaanza kumpa Uzia ushuru.[z] Mwishowe sifa[a] yake ikaenea mpaka Misri, kwa kuwa

SURA 25
a 1Fa 12:15; 2Nya 22:7
b 2Nya 25:14
c 2Fa 14:11
d 2Sa 2:14; 2Nya 25:17
e Yos 21:16; 1Sa 6:9; 1Sa 6:19
f 2Fa 14:12
g 1Fa 22:36
h Met 25:8
i 2Fa 14:13
j Ne 8:16; Ne 12:39
k 2Nya 26:9; Yer 31:38; Zek 14:10
l 1Fa 7:51; 1Fa 15:18; 2Fa 25:15; 2Nya 12:9
m 1Fa 14:26; 2Fa 24:13
n 2Fa 14:14
o 2Fa 14:1
p 2Fa 13:10; 2Fa 14:15; 2Fa 14:17
q 2Nya 12:15
r 1Fa 14:29; 2Fa 12:19
s 2Fa 14:18
t 2Fa 12:20; 2Fa 15:10; 2Fa 21:23
u Yos 10:31; Mik 1:13

Safu ya 2
a 2Fa 14:19
b 2Fa 14:20
c 1Fa 2:10; 1Fa 11:43

SURA 26
d 2Nya 33:25
e 2Fa 15:13; Mt 1:8
f 2Fa 21:24
g 2Fa 14:21
h 1Fa 9:26; 2Fa 16:6; 2Nya 8:17
i 2Fa 14:22
j Isa 1:1; Isa 6:1
k 2Fa 15:2
l 2Fa 12:2
m 2Fa 14:3
n Kum 4:29; 2Nya 14:7; 2Nya 17:4
o Mwa 18:19
p 1Fa 3:13; Zb 1:3; Met 10:22
q 2Sa 8:1; 2Nya 21:16; Isa 14:29
r 1Nya 18:1
s Yos 15:11
t Yos 13:3; 1Sa 5:1
u Yos 15:46

v 1Nya 5:20; 2Nya 14:11; Zb 33:20; Mdo 26:22; w 2Nya 17:11; x 1Nya 4:41; y Mwa 19:38; Amu 11:15; z 2Sa 8:6; 1Nya 18:6; a Mwa 12:2.

alionyesha nguvu kwa kiwango kisicho cha kawaida. **9** Zaidi ya hayo, Uzia akajenga minara[a] katika Yerusalemu kando ya Lango la Pembeni[b] na kando ya Lango la Bonde[c] na kando ya Nguzo, naye akaitia nguvu. **10** Tena akajenga minara[d] nyikani, na kuchimba matangi mengi ya maji (kwa maana alikuwa na mifugo mingi sana), na pia katika Shefela[e] na katika nchi tambarare ya juu. Palikuwa na wakulima na watunzamizabibu katika milima na katika Karmeli, kwa maana alipenda kilimo.

11 Tena Uzia akawa na jeshi la kupigana vita, wale wanaoingia katika utumishi wa kijeshi vikosi vikosi,[f] kulingana na hesabu ya uandikisho[g] wao kwa mkono wa Yeieli mwandishi[h] na Maaseya ofisa aliye chini ya[i] Hanania mmoja wa wakuu wa mfalme.[j] **12** Hesabu kamili ya vichwa vya nyumba za ukoo wa upande wa baba,[k] ya mashujaa,[l] wanaume wenye nguvu,[m] ilikuwa elfu mbili na mia sita. **13** Na chini ya amri yao majeshi yalikuwa ni watu mia tatu na saba elfu na mia tano wa kupigana vita wakiwa na nguvu za kijeshi ili kumsaidia mfalme kupigana na adui.[n] **14** Na Uzia akaendelea kuwafanyia matayarisho, jeshi lote, ngao[o] na mikuki[p] na kofia[q] na mavazi ya chuma[r] na pinde[s] na mawe ya kombeo.[t] **15** Tena akatengeneza mitambo ya vita katika Yerusalemu, ubuni wa mafundi, ili iwekwe juu ya minara[u] na juu ya sehemu za pembeni, ili irushe mishale na mawe makubwa. Basi sifa[v] yake ikaenea mbali sana, kwa kuwa alisaidiwa kwa njia ya ajabu mpaka akawa na nguvu.

SURA 26

a 2Nya 14:7
b 2Fa 14:13
Yer 31:38
Zek 14:10
c Ne 3:13
d 2Fa 9:17
e 1Nya 27:28
f 1Nya 12:18
g Hes 1:3
2Sa 24:9
h 1Nya 27:32
2Nya 24:11
i 1Nya 26:28
j 1Nya 28:1
k 1Nya 27:1
l 1Nya 5:24
1Nya 12:21
m 1Nya 26:6
n 2Nya 11:1
2Nya 13:3
2Nya 17:14
o 2Nya 17:17
p 2Nya 11:12
2Nya 14:8
2Nya 25:5
q 1Sa 17:5
Yer 46:4
r 1Sa 17:38
s 1Nya 12:2
t Amu 20:16
1Sa 17:49
u 2Nya 14:7
v 1Fa 4:31

Safu ya 2

a Kum 32:15
b Met 29:23
1Pe 5:5
c Hes 1:51
d Met 28:1
e Hes 16:40
Hes 18:7
Met 21:24
f Kut 30:7
1Nya 23:13
Ebr 5:4
g Hes 3:10
Hes 18:7
1Sa 2:30
h 2Nya 16:10
2Nya 25:16
i Kut 30:7
j Hes 12:10
2Fa 5:27
k Law 13:2
l Law 13:3
Kum 24:8
Met 11:2
m Law 14:34
Kum 28:22
Kum 28:35
n 2Fa 15:5

16 Hata hivyo, mara tu alipopata nguvu, moyo wake ukawa na majivuno[a] hata kufikia hatua ya kusababisha uharibifu,[b] hivi kwamba akatenda kwa ukosefu wa uaminifu kwa Yehova Mungu wake, akaingia katika hekalu la Yehova ili kufukiza uvumba juu ya madhabahu ya uvumba.[c] **17** Mara moja Azaria kuhani na makuhani wa Yehova pamoja naye, wanaume mashujaa 80, wakaingia nyuma yake. **18** Kisha wakasimama kumpinga Uzia mfalme[d] na kumwambia: "Si kazi yako,[e] Ee Uzia, kumfukizia Yehova uvumba, bali ni kazi ya makuhani, wana wa Haruni,[f] waliotakaswa, kufukiza uvumba. Ondoka ndani ya patakatifu; kwa maana umetenda kwa ukosefu wa uaminifu, wala jambo hilo si utukufu[g] wowote kwako mbele za Yehova Mungu."

19 Lakini Uzia akawa na ghadhabu,[h] huku mkononi mwake akiwa na chetezo,[i] cha kufukiza uvumba, na, alipokuwa na ghadhabu juu ya makuhani, ukoma[j] ukatokea[k] katika paji la uso wake mbele ya wale makuhani katika nyumba ya Yehova kando ya madhabahu ya uvumba. **20** Wakati Azaria yule mkuu wa makuhani na makuhani wote walipogeuka kumwelekea, tazama, alikuwa amepigwa na ukoma katika paji la uso wake![l] Kwa hiyo wakaanza kumtoa hapo upesi, naye mwenyewe pia akafanya haraka kutoka nje, kwa sababu Yehova alikuwa amempiga.[m]

21 Na Uzia[n] mfalme akaendelea kuwa mwenye ukoma mpaka siku ya kufa kwake, naye akaendelea kukaa katika nyumba fulani akiwa ameondolewa wajibu wake, akiwa

mwenye ukoma;[a] kwa sababu
alikuwa ametengwa na nyu-
mba ya Yehova, huku Yotha-
mu mwana wake akiwa juu ya
nyumba ya mfalme, akiwahu-
kumu watu wa nchi.
22 Na yale mambo mengine
ya Uzia,[b] ya kwanza na ya mwi-
sho, Isaya[c] mwana wa Amozi[d]
nabii ameyaandika. **23** Mwi-
showe Uzia akalala pamoja na
mababu zake; na kwa hiyo wa-
kamzika pamoja na mababu
zake, lakini katika uwanja wa
kuzikia wa wafalme,[e] kwa maa-
na walisema: "Yeye ni mwenye
ukoma." Na Yothamu[f] mwana
wake akaanza kutawala maha-
li pake.

27 Yothamu[g] alikuwa na
umri wa miaka 25 alipo-
anza kutawala, naye akatawala
miaka 16 katika Yerusalemu. Na
jina la mama yake lilikuwa Ye-
rusha[h] binti ya Sadoki. **2** Naye
akaendelea kufanya yaliyokuwa
sawa machoni pa Yehova,[i] ku-
lingana na yote ambayo Uzia
baba yake alikuwa amefanya.[j]
Ila tu hakulivamia hekalu la Ye-
hova.[k] Hata hivyo, watu bado
walikuwa wakitenda kwa uhari-
bifu.[l] **3** Yeye alijenga lango la
juu[m] la nyumba ya Yehova, naye
akafanya ujenzi mkubwa katika
ukuta wa Ofeli.[n] **4** Naye
akajenga majiji[o] katika eneo
lenye milima la Yuda,[p] akaje-
nga ngome[q] na minara[r] msitu-
ni.[s] **5** Naye akapigana vita na
mfalme wa wana wa Amoni,[t] na
mwishowe akawa na nguvu ku-
liko wao, hivi kwamba wana wa
Amoni wakampa mwaka huo ta-
lanta mia moja za fedha na vi-
pimo[u] elfu kumi vya ngano[v] na
elfu kumi vya shayiri.[w] Wana
wa Amoni walimlipa vitu hi-
vyo, pia katika mwaka wa pili
na wa tatu.[x] **6** Basi Yothamu
akaendelea kujitia nguvu, kwa
maana alitayarisha njia zake
mbele za Yehova Mungu wake.[a]
7 Na yale mambo mengine ya
Yothamu[b] na vita vyake vyo-
te na njia zake, tazama, yamea-
ndikwa katika Kitabu[c] cha Wa-
falme wa Israeli na wa Yuda.
8 Alikuwa na umri wa mia-
ka 25 alipoanza kutawala, naye
akatawala miaka 16 katika Ye-
rusalemu.[d] **9** Mwishowe Yo-
thamu akalala pamoja na ma-
babu zake,[e] nao wakamzika ka-
tika Jiji la Daudi.[f] Na Ahazi[g]
mwana wake akaanza kutawala
mahali pake.

28 Ahazi[h] alikuwa na umri
wa miaka 20 alipoanza
kutawala, naye akatawala mia-
ka 16 katika Yerusalemu,[i] naye
hakufanya yaliyokuwa sawa
machoni pa Yehova kama Da-
udi babu yake.[j] **2** Bali alite-
mbea katika njia za wafalme wa
Israeli,[k] na hata akatengene-
za sanamu za kuyeyushwa[l] za
Mabaali.[m] **3** Naye akafukiza
moshi wa dhabihu[n] katika bo-
nde la mwana wa Hinomu,[o] aka-
teketeza wanawe[p] katika moto,
kulingana na machukizo[q] ya
mataifa ambayo Yehova aliku-
wa ameyafukuza kutoka mbe-
le ya wana wa Israeli.[r] **4** Naye
alitoa dhabihu kwa ukawaida[s]
na kufukiza moshi wa dhabihu
katika mahali pa juu na juu[t] ya
vilima[u] na chini ya kila namna
ya mti wenye majani mengi.[v]
5 Kwa hiyo Yehova Mungu
wake akamtia mkononi[w] mwa
mfalme wa Siria,[x] nao wakampi-
ga na kuchukua kutoka kwa-
ke hesabu kubwa ya mate-
ka na kuwaleta Damasko.[y] Naye

SURA 26
a Law 13:46; Hes 5:2; Hes 12:14; Hes 12:15; 2Fa 7:3
b 2Fa 15:6
c Isa 6:1
d Isa 1:1
e 2Fa 15:7
f 2Fa 15:32

SURA 27
g 1Nya 3:12; Isa 1:1; Ho 1:1; Mik 1:1; Mt 1:9
h 2Fa 15:33
i 2Fa 12:2; 2Nya 17:3
j 2Fa 15:34; 2Nya 26:4
k 2Nya 26:16; Zb 119:120
l 2Fa 15:35
m Yer 20:2
n 2Nya 33:14; Ne 3:26
o 2Nya 11:5; 2Nya 14:7
p Yos 14:12
q 2Nya 17:12
r 2Fa 9:17; 2Nya 26:10
s 1Sa 23:15
t Amu 11:4; 2Sa 10:1; 2Nya 20:1; Yer 49:1
u 2Nya 2:10
v 1Fa 5:11
w Kum 8:8; 2Nya 2:15
x 2Nya 26:8

Safu ya 2
a 2Nya 19:3; 2Nya 26:5
b 2Fa 15:36
c 2Fa 8:23; 2Fa 12:19
d 2Fa 15:33
e 2Sa 7:12
f 2Sa 5:9; 1Fa 14:31
g 2Fa 15:38

SURA 28
h 2Fa 16:2; 1Nya 3:13; Isa 7:1; Ho 1:1; Mik 1:1; Mt 1:9
i 2Fa 16:2
j 1Fa 3:14
k 1Fa 12:28; 1Fa 16:33
l Kut 34:17; Law 19:4
m Amu 2:11
n Ho 2:13
o 2Fa 23:10; Yer 7:31
p 2Nya 33:6
q Kum 12:31; 2Fa 21:2; 2Nya 33:2; r 2Fa 16:3; s 2Fa 16:4; t Law 26:30; u 1Fa 14:23; v Isa 57:5; w Amu 2:14; 2Nya 33:11; 2Nya 36:17; Zb 76:12; x 2Fa 16:6; 2Nya 24:24; y Mwa 14:15; 2Sa 8:6; 1Nya 18:5.

pia akatiwa mkononi mwa mfalme wa Israeli,[a] naye akampiga kwa mauaji makubwa.
6 Basi Peka[b] mwana wa Remalia[c] akaua katika Yuda watu 120,000 katika siku moja, wote wakiwa ni wanaume mashujaa, kwa sababu walimwacha Yehova[d] Mungu wa mababu zao. **7** Tena, Zikri, mwanamume mwenye nguvu wa Efraimu,[e] akamuua Maaseya mwana wa mfalme na Azrikamu kiongozi wa nyumba na Elkana yule aliyekuwa wa pili kwa mfalme. **8** Na tena wana wa Israeli wakawachukua mateka ndugu zao mia mbili elfu, wanawake, wana na mabinti; na pia wakapora nyara nyingi kutoka kwao, kisha wakaleta nyara hizo Samaria.[f]

9 Na palikuwa na nabii wa Yehova hapo ambaye jina lake lilikuwa Odedi. Basi akaenda mbele ya jeshi lililokuwa likija Samaria na kuwaambia: "Tazama! Yehova Mungu wa mababu zenu aliwatia hao mkononi mwenu kwa sababu ya ghadhabu[g] yake juu ya Yuda, hivi kwamba mkafanya mauaji kati yao kwa ghadhabu[h] ambayo imefika mpaka mbinguni.[i] **10** Na sasa mnafikiria kuwafanya wana wa Yuda na wana wa Yerusalemu kuwa watumishi[j] na wajakazi wenu. Hata hivyo, je, ninyi wenyewe hamna visa vya hatia juu ya Yehova Mungu wenu? **11** Na sasa nisikilizeni, na mwarudishe mateka ambao mmewateka kutoka kwa ndugu zenu,[k] kwa maana hasira ya Yehova inayowaka iko juu yenu."[l]

12 Ndipo watu fulani wa vichwa[m] vya wana wa Efraimu,[n] Azaria mwana wa Yehohanani, Berekia mwana wa Meshilemothi na Yehizkia mwana wa Shalumu na Amasa mwana wa Hadlai, wakasimama kuwapinga wale waliokuwa wakiingia kutoka katika shughuli hiyo ya kijeshi, **13** nao wakawaambia: "Msiingize mateka humu, kwa sababu tutakuwa na hatia juu ya Yehova. Mnafikiria kuziongeza dhambi zetu na hatia yetu, kwa maana sisi tuna hatia kubwa,[a] na kuna hasira inayowaka[b] juu ya Israeli."
14 Basi wale watu wenye silaha[c] wakawaacha wale mateka[d] na ile nyara mbele ya wakuu[e] na kutaniko lote. **15** Kisha watu waliochaguliwa kwa majina[f] yao wakasimama na kuwachukua wale mateka, na wote waliokuwa uchi wakawavika nguo kutokana na zile nyara. Basi wakawavika[g] na kuwapa viatu, wakawalisha[h] na kuwapa vinywaji[i] na kuwapaka mafuta. Tena, kuhusu wowote wenye kutetemeka, wakawasafirisha[j] juu ya punda na kuwaleta Yeriko,[k] jiji la mitende,[l] kando ya ndugu zao. Kisha wakarudi Samaria.[m]

16 Wakati huo Mfalme Ahazi[n] akatuma ujumbe kwa wafalme wa Ashuru[o] ili wamsaidie.
17 Na kwa mara nyingine tena Waedomu[p] wakaingia na kuwapiga Yuda na kuchukua mateka. **18** Nao Wafilisti[q] wakavamia majiji ya Shefela[r] na Negebu[s] katika Yuda na kuteka Beth-shemeshi[t] na Aiyaloni[u] na Gederothi[v] na Soko[w] na miji yake ya kandokando na Timna[x] na miji yake ya kandokando na Gimzo na miji yake ya kandokando; nao wakaanza kukaa humo. **19** Kwa kuwa Yehova alinyenyekeza[y] Yuda kwa sababu ya Ahazi mfalme wa Israeli, kwa sababu aliachilia mambo katika Yuda,[z] nao wakatenda

SURA 28

a 2Fa 16:5
b 2Fa 15:37
Isa 7:1
c Isa 7:9
d Kum 6:14
Kum 31:16
2Nya 15:2
Zb 73:27
Isa 1:28
Yer 2:19
e Isa 9:21
f 1Fa 16:24
1Fa 22:51
g Amu 3:8
Zb 69:26
Isa 10:5
Zek 1:15
h Eze 25:12
i Mwa 4:10
Ezr 9:6
Ufu 18:5
j Law 25:39
Law 25:46
2Nya 8:9
k Isa 58:6
Yer 34:15
l Mt 7:2
Yak 2:13
m 1Nya 28:1
n Isa 9:21

Safu ya 2

a Hes 32:14
b Kut 22:24
Yos 22:18
Ro 2:5
c 1Nya 12:23
d 2Nya 28:8
e 1Nya 28:1
Mhu 12:11
f 2Nya 28:12
g Ayu 31:19
Zb 106:46
Isa 58:7
h 2Fa 6:22
Yak 2:15
i Lu 6:27
Ro 12:20
j Ro 15:1
k Hes 22:1
Yos 6:1
l Kum 34:3
Amu 1:16
m 1Fa 16:24
n 2Fa 16:7
Isa 7:10
o Isa 7:17
p Law 26:18
Oba 10
q 1Sa 5:1
1Sa 31:11
2Nya 26:6
r Kum 1:7
Yos 9:1
2Nya 26:10
s Hes 21:1
Kum 34:3
2Sa 24:7
t Yos 15:10
1Sa 6:9
u 2Nya 11:10
v Yos 15:41
w Yos 15:35
x Amu 14:1
y Law 26:18
Kum 28:43
1Sa 2:7
Ayu 40:12
z Kut 32:25

kwa ukosefu mkubwa sana wa
uaminifu kumwelekea Yehova.
20 Mwishowe Tilgath-pilne-
seri[a] mfalme wa Ashuru aka-
ja kupigana naye na kumtaa-
bisha,[b] naye hakumtia nguvu.
21 Kwa kuwa Ahazi alichukua
mali yote katika nyumba ya Ye-
hova[c] na nyumba ya mfalme[d]
na ya wakuu[e] na kumpa za-
wadi mfalme wa Ashuru;[f] la-
kini jambo hilo halikumsai-
dia kamwe. **22** Hata hivyo,
wakati alipokuwa akimtaabi-
sha, yeye, yaani, Mfalme Aha-
zi, alizidi kutenda kwa uko-
sefu wa uaminifu kumwele-
kea Yehova.[g] **23** Naye akaa-
nza kuitolea dhabihu miungu[h]
ya Damasko[i] iliyokuwa ikimpi-
ga, naye akasema: "Kwa saba-
bu miungu ya wafalme wa Siria
inawasaidia wao,[j] mimi nitaito-
lea dhabihu, ili inisaidie."[k] Nayo
ikawa kisababishi cha kumfa-
nya yeye na Israeli wote waji-
kwae.[l] **24** Zaidi ya hayo, Aha-
zi akavikusanya vyombo[m] vya
nyumba ya Mungu wa kweli na
kuvikata vipande-vipande vyo-
mbo vya nyumba ya Mungu
wa kweli,[n] akaifunga milango[o]
ya nyumba ya Yehova, akaji-
tengenezea madhabahu kati-
ka kila pembe katika Yerusale-
mu.[p] **25** Na katika majiji yote,
majiji ya Yuda, akajenga ma-
hali pa juu[q] kwa ajili ya kui-
fukizia miungu mingine moshi
wa uvumba,[r] hivi kwamba aka-
mtia uchungu[s] Yehova Mungu
wa mababu zake.
26 Na yale mambo yake me-
ngine[t] na njia zake, ya kwa-
nza na ya mwisho, tazama, ya-
meandikwa katika Kitabu[u] cha
Wafalme wa Yuda na wa Israe-
li. **27** Mwishowe Ahazi akala-
la pamoja na mababu zake, nao
wakamzika katika jiji, Yerusa-

SURA 28
a 2Fa 15:29
2Fa 16:7
1Nya 5:26
b 2Fa 17:5
Isa 7:20
c 2Nya 12:9
d 2Fa 18:15
e 1Nya 28:1
f 2Fa 18:16
g Zb 52:7
Met 19:3
h 2Nya 25:14
Yer 44:5
i 2Fa 16:12
2Fa 16:13
j Hab 1:11
k Yer 10:5
Yer 44:18
l Kut 23:33
Kum 7:16
Isa 1:28
m 1Fa 7:45
2Nya 4:18
n 2Fa 16:17
o 1Fa 6:34
2Nya 29:7
p 2Nya 33:5
Yer 2:28
q 1Fa 14:23
2Fa 15:35
2Nya 21:11
2Nya 33:3
r 2Nya 28:4
s 1Ko 10:22
t 2Nya 27:7
u 2Fa 16:19

Safu ya 2
a 2Nya 21:20
2Nya 33:20
Met 10:7

SURA 29
b 2Fa 18:1
Isa 1:1
Ho 1:1
Mt 1:10
c 2Fa 18:2
d 2Nya 31:20
Met 10:9
e 1Fa 3:14
1Fa 15:5
2Fa 18:3
f 1Fa 6:34
2Nya 28:24
g 2Nya 32:6
h Kut 19:15
1Nya 15:12
i 2Fa 18:4
Eze 8:3
j 2Nya 28:23
2Nya 34:21
Ezr 5:12
Ne 9:16
k Yer 44:21
l Yer 2:13
m Yer 2:27
Eze 8:16
n 1Fa 6:34
o Law 24:2
p Kut 30:8
2Nya 13:11
q Kut 29:38
Mal 1:10
r Kum 28:15
2Nya 24:18
s Kum 28:25
t Law 26:32
u 1Fa 9:8
Yer 18:16

lemu, kwa maana hawakumpe-
leka kwenye makaburi ya wa-
falme wa Israeli.[a] Na Hezekia
mwana wake akaanza kutawa-
la mahali pake.
29 Hezekia[b] alikuwa mfalme
akiwa na umri wa miaka
25, naye akatawala miaka 29 ka-
tika Yerusalemu. Na jina la mama
yake lilikuwa Abiya binti ya Ze-
karia.[c] **2** Naye akaendelea ku-
fanya yaliyokuwa sawa macho-
ni pa Yehova,[d] kulingana na yote
ambayo Daudi babu yake aliku-
wa amefanya.[e] **3** Yeye mwenye-
we, katika mwaka wa kwanza
wa kutawala kwake, katika mwe-
zi wa kwanza, aliifungua mila-
ngo ya nyumba ya Yehova
na kuanza kuirekebisha.[f] **4** Ki-
sha akawaleta makuhani na Wa-
lawi na kuwakusanya mahali pa-
lipo wazi[g] upande wa mashariki.
5 Naye akawaambia: "Nisikilize-
ni, enyi Walawi. Sasa jitakasen-
i[h] na mwitakase nyumba ya Ye-
hova Mungu wa mababu zenu,
na mwondoe kitu kichafu kuto-
ka mahali patakatifu.[i] **6** Kwa
maana baba zetu wametenda
kwa ukosefu wa uaminifu[j] nao
wametenda mabaya machoni pa
Yehova Mungu wetu,[k] hivi
kwamba walimwacha[l] na ku-
geuza nyuso zao kutoka kwe-
nye maskani ya Yehova[m] na ku-
mpa visogo vyao. **7** Pia walifu-
nga milango[n] ya ukumbi na ku-
zima taa,[o] nao hawakufukiza
uvumba,[p] wala hawakumtolea
Mungu wa Israeli dhabihu ya ku-
teketezwa katika mahali pataka-
tifu.[q] **8** Na ghadhabu[r] ya Yeho-
va ikaja juu ya Yuda na Yeru-
salemu, hivi kwamba akawafa-
nya kuwa kitu cha kutetemesha
watu,[s] kitu cha kushangaza[t] na
kisababishi cha kupiga mluzi,[u]
kama vile mnavyoona kwa ma-
cho yenu wenyewe. **9** Na ta-

zama, mababu zetu walianguka kwa upanga,[a] na wana wetu
na binti zetu na wake zetu
walikuwa utekwani kwa sababu ya
hayo.[b] **10** Sasa ninataka moyo-
ni mwangu kufanya agano[c] pa-
moja na Yehova Mungu wa Isra-
eli, ili hasira yake inayowaka
igeuke kutoka kwetu. **11** Sasa,
wanangu, msijipumzishe,[d] kwa
maana Yehova amewachagua ni-
nyi msimame mbele zake ili ku-
mhudumia[e] na kuwa wahudumu[f]
wake na kuwa wenye kufukiza
moshi wa dhabihu."[g]

12 Ndipo Walawi[h] wakasi-
mama, Mahathi mwana wa
Amasai na Yoeli mwana wa
Azaria wa wana wa Wakohathi;[i]
na kutoka kwa wana wa Me-
rari,[j] Kishi mwana wa Abdi
na Azaria mwana wa Yehale-
leli; na kutoka kwa Wagersho-
ni,[k] Yoa mwana wa Zima na
Edeni mwana wa Yoa; **13** na
kutoka kwa wana wa Elisafa-
ni,[l] Shimri na Yeueli; na kuto-
ka kwa wana wa Asafu,[m] Zeka-
ria na Matania; **14** na kutoka
kwa wana wa Hemani,[n] Yehieli
na Shimei; na kutoka kwa wana
wa Yeduthuni,[o] Shemaya na
Uzieli. **15** Ndipo wakawaku-
sanya ndugu zao na kujitakasa[p]
na kuja kulingana na amri ya
mfalme kwa maneno[q] ya Yeho-
va, ili kuitakasa[r] nyumba ya Ye-
hova. **16** Sasa makuhani wa-
kaingia ndani ya nyumba ya Ye-
hova ili kufanya utakaso, nao
wakauondoa uchafu wote wali-
oupata katika hekalu la Yehova
mpaka kwenye ua[s] wa nyumba
ya Yehova. Nao Walawi wakau-
chukua ili waupeleke nje kati-
ka bonde la mto la Kidroni[t] upa-
nde wa nje. **17** Basi wakaa-
nza kutakasa katika siku ya
kwanza ya mwezi wa kwanza,
na katika siku ya nane ya mwe-
zi huo wakaja katika ukumbi[a]
wa Yehova; nao wakaitakasa
nyumba ya Yehova katika siku
nane, na katika siku ya kumi na
sita ya mwezi wa kwanza[b] wa-
kamaliza.

18 Kisha wakaingia kwa He-
zekia mfalme na kusema: "Tu-
meitakasa nyumba yote ya Ye-
hova, madhabahu[c] ya toleo la
kuteketezwa na vyombo[d] vya-
ke vyote, na meza[e] ya mka-
te wa tabaka na vyombo vyake
vyote.[f] **19** Nasi tumetayari-
sha vyombo[g] vyote ambavyo
Mfalme Ahazi[h] aliondoa kati-
ka utumishi wakati wa utawala
wake katika ukosefu wake wa
uaminifu,[i] nasi tumevitakasa;[j]
na tazama, viko mbele ya ma-
dhabahu ya Yehova."

20 Naye Hezekia[k] mfalme
akaondoka mapema,[l] akawa-
kusanya wakuu[m] wa jiji, na
kupanda kwenda katika nyu-
mba ya Yehova. **21** Nao wa-
kaleta ng'ombe-dume saba[n] na
kondoo-dume saba na wana-kon-
doo dume saba na mbuzi-
dume saba wawe toleo la dha-
mbi[o] kwa ajili ya ufalme na kwa
ajili ya patakatifu na kwa aji-
li ya Yuda. Basi akawaambia
wana wa Haruni, makuhani,[p]
wawatoe wawe toleo juu ya ma-
dhabahu ya Yehova. **22** Kwa
hiyo wakawachinja[q] wale ng'o-
mbe na makuhani wakapokea
damu[r] na kuinyunyiza[s] juu ya
madhabahu; kisha wakawachi-
nja wale kondoo-dume[t] na kui-
nyunyiza damu[u] juu ya ma-
dhabahu, nao wakawachinja
wana-kondoo na kuinyunyi-
za damu juu ya madhabahu.
23 Kisha wakawaleta karibu
wale mbuzi-dume[v] wa toleo la
dhambi mbele ya mfalme na ku-
taniko na kuweka mikono yao
juu yao.[w] **24** Sasa makuhani

SURA 29

a Law 26:17
b 2Nya 28:5
c 2Nya 15:12
d Yoh 5:17
1Ko 15:58
e Hes 3:6
Hes 18:2
Hes 18:6
Kum 10:8
Lu 12:48
f 1Nya 15:2
1Nya 23:13
2Nya 13:10
g Hes 16:40
Hes 18:7
h 1Nya 23:3
i Hes 4:2
1Nya 15:5
1Nya 23:12
j 1Nya 15:6
1Nya 23:21
k 1Nya 15:7
1Nya 23:7
l 1Nya 15:8
m 1Nya 15:17
1Nya 25:2
n 1Nya 25:5
o 1Nya 25:1
1Nya 25:6
p 2Nya 29:5
q 2Nya 30:12
r 1Nya 23:28
s 1Fa 6:36
t 2Fa 23:4
2Fa 23:6
2Nya 15:16
Yoh 18:1

Safu ya 2

a 1Fa 6:3
1Nya 28:11
2Nya 3:4
b Kut 12:2
c 2Nya 4:1
d 1Fa 7:40
2Nya 4:11
e 1Fa 7:48
2Nya 4:8
2Nya 13:11
f 1Fa 7:50
g 2Nya 28:24
h 2Nya 28:1
i 2Nya 28:2
2Nya 28:25
j 2Nya 29:5
k 2Fa 18:1
Mt 1:10
l Kut 24:4
Yos 6:12
m 1Nya 28:1
n 1Nya 15:26
o Law 4:3
Law 4:14
Hes 15:22
Hes 15:24
p Hes 18:1
q Law 3:2
Law 4:4
Law 8:15
r Law 4:7
s Law 1:5
Law 4:18
Ebr 9:21
t Law 8:18
u Law 8:19
v Law 9:15
w Law 1:4
Law 4:15

wakawachinja na kutoa toleo la
dhambi kwa damu yao juu ya
madhabahu, ili kufanya upata-
nisho kwa ajili ya Israeli wote;[a]
kwa sababu mfalme alisema to-
leo la kuteketezwa na toleo la
dhambi liwe[b] kwa ajili ya Israe-
li[c] wote.
25 Wakati huohuo akawa-
weka Walawi[d] katika nyumba
ya Yehova, wakiwa na matoa-
zi,[e] na vinanda[f] na vinubi,[g] ku-
lingana na amri ya Daudi[h] na
ya Gadi[i] mwonaji wa mfalme
na ya nabii Nathani,[j] kwa maa-
na amri hiyo ilikuwa kulinga-
na na mkono wa Yehova ku-
pitia manabii wake.[k] **26** Basi
Walawi wakaendelea kusima-
ma wakiwa na vyombo[l] vya Da-
udi, na pia makuhani wakiwa
na tarumbeta.[m]
27 Ndipo Hezekia akasema
dhabihu ya kuteketezwa itole-
we juu ya madhabahu; na waka-
ti lile toleo la kuteketezwa lili-
poanza, wimbo[n] wa Yehova uka-
anza na pia tarumbeta, chi-
ni ya mwelekezo wa vyombo
vya Daudi mfalme wa Israe-
li. **28** Na kutaniko lote waka-
inama[o] huku wimbo ukivuma[p]
na tarumbeta zikipigwa—hayo
yote yakaendelea mpaka lile to-
leo la kuteketezwa lilipomaliziki-
ka. **29** Na mara tu walipoma-
liza kulitoa, mfalme na wote
waliokuwa pamoja naye waka-
inama na kusujudu.[q] **30** Sasa
Hezekia mfalme na wakuu[r] wa-
kawaambia Walawi wamsifu Ye-
hova kwa maneno ya Daudi[s] na
ya Asafu[t] yule mwonaji. Kwa
hiyo wakaanza kutoa sifa kwa
kushangilia,[u] wakaendelea kui-
nama na kusujudu.[v]
31 Mwishowe Hezekia akaji-
bu na kusema: "Sasa mmeuja-
za[w] mkono wenu nguvu kwa aji-
li ya Yehova. Karibieni, mlete
dhabihu[a] na dhabihu za shukra-
ni[b] katika nyumba ya Yehova."
Nalo kutaniko likaanza kuleta
dhabihu na dhabihu za shukra-
ni, na pia kila mtu aliyeku-
wa na moyo wa kupenda, aka-
leta matoleo ya kuteketezwa.[c]
32 Na hesabu ya matoleo ya
kuteketezwa ambayo kutani-
ko hilo lilileta ikawa ng'ombe
70, kondoo-dume 100, wana-ko-
ndoo dume 200—hao wote wa-
kiwa ni toleo la kuteketezwa
kwa Yehova;[d] **33** na pia mato-
leo matakatifu, ng'ombe 600 na
wanyama 3,000 kati ya kundi.
34 Ila tu makuhani[e] walikuwa
wachache mno, nao hawakuwe-
za kuchuna ngozi yale mato-
leo yote ya kuteketezwa.[f] Kwa
hiyo ndugu[g] zao Walawi waka-
wasaidia mpaka kazi ilipoisha[h]
na mpaka makuhani walipoku-
wa wamejitakasa,[i] kwa kuwa
Walawi walikuwa wanyoofu[j] za-
baada ya siku naye hakuwasikiliza, wakamwambia Hamani ili kuona kama mambo
yake Mordekai yangevumiliwa;[i] maana alikuwa amewaambia kuwa yeye ni Myahudi.[j]
5 Basi Hamani akazidi kuona kwamba Mordekai hakuwa akiinama wala kumsujudia,[k] naye Hamani akajawa na
ghadhabu.[l] **6** Lakini lilikuwa jambo la kudharaulika machoni pake kunyoosha mkono wake juu ya Mordekai peke
yake, kwa maana walikuwa wamemwambia kuhusu watu wa
Mordekai; kwa hiyo Hamani
akaanza kutafuta kuwaangamiza[m] Wayahudi wote waliokuwa katika utawala wote wa
Ahasuero, watu wa Mordekai.[n]
7 Katika mwezi wa kwanza,[o] yaani, mwezi wa Nisani, katika mwaka wa kumi na
mbili[p] wa Mfalme Ahasuero,
mtu fulani alipiga Puri,[q] yaani,

SURA 2

a Ezr 4:15
Est 6:1

SURA 3

b Est 3:10
Est 8:7
Est 9:24
c Hes 24:7
1Sa 15:8
1Sa 15:32
d Zb 12:8
e Est 1:14
f Est 2:19
g Kut 17:14
Kut 17:16
Kum 25:19
1Sa 15:3
Zb 139:21
h Mdo 5:29
i Da 6:13
j Ne 1:2
Est 2:5
k Est 3:2
l Est 5:9
Met 12:16
Met 27:3
m Zb 73:6
Zb 83:4
n Est 9:20
o Kut 12:2
Kut 34:18
p Est 1:3
Est 2:16
q Est 9:24

Safu ya 2

a Yoe 3:3
Oba 11
Mt 27:35
b Est 9:1
c Kum 4:27
Kum 30:3
Ne 1:8
Yer 50:17
Zek 7:14
Yak 1:1
d Est 1:1
e Zb 94:21
f Mt 18:24
g Est 9:3
h Mwa 41:42
Est 8:2
Da 6:17
i Est 3:1
j Hes 24:7
1Sa 15:8
k Est 7:6
Est 9:24
l Est 4:7
m Met 29:12
Yer 40:4
n Est 8:9
o Zb 94:20
Da 6:8
p Est 1:1
Da 6:1
q Est 1:22
r Da 6:15
s Mwa 41:42
Est 8:8
Da 6:17

Kura,[a] mbele ya Hamani siku
baada ya siku na mwezi baada ya mwezi, mpaka mwezi wa
kumi na mbili, yaani, mwezi
wa Adari.[b] **8** Ndipo Hamani
akamwambia Mfalme Ahasuero: "Kuna kikundi fulani cha
watu waliotawanyika[c] na kujitenga kati ya vikundi vya watu
katika wilaya zote za utawala wako;[d] na sheria zao ni tofauti na zile za watu wengine
wote, nao hawatendi sheria za
mfalme,[e] na haifai kwa mfalme
kuwaachilia. **9** Mfalme akiona vema, na iandikwe kwamba
waharibiwe; nami nitalipa talanta elfu kumi[f] za fedha mikononi mwa wale wanaofanya
kazi[g] hiyo kwa kuzileta katika
hazina ya mfalme."

10 Kwa hiyo mfalme akavua
pete yake ya muhuri[h] kutoka mkononi mwake na kumpa
Hamani[i] mwana wa Hamedatha Mwagagi,[j] yule mwenye kuwaonyesha Wayahudi uadui.[k]
11 Tena mfalme akamwambia
Hamani: "Umepewa fedha,[l] pia
watu, ili uwafanyie kulingana
na yaliyo mema machoni pako
mwenyewe."[m] **12** Ndipo waandishi[n] wa mfalme wakaitwa
katika mwezi wa kwanza siku
ya kumi na tatu ya mwezi huo.
Basi kuandika[o] kukaendelea
kulingana na yote ambayo Hamani aliwaamuru maliwali wa
mfalme na magavana waliokuwa juu ya wilaya mbalimbali za
utawala,[p] na wakuu wa vikundi
mbalimbali vya watu, wa kila
wilaya ya utawala, katika mtindo wao wa kuandika,[q] na kila
kikundi cha watu kwa lugha
yao wenyewe. Hayo yaliandikwa kwa jina[r] la Mfalme Ahasuero na kutiwa muhuri kwa
pete[s] ya mfalme.

13 Na barua zikapelekwa
kwa mkono wa wajumbe[a]
kwa wilaya zote za utawala wa
mfalme, ili kuangamiza, kuua
na kuharibu Wayahudi wote,
vijana kwa wazee, watoto kwa
wanawake, katika siku moja,[b]
siku ya kumi na tatu ya mwezi
wa kumi na mbili, yaani, mwe-
zi wa Adari,[c] na kuteka nya-
ra na kuwapora.[d] **14** Nakala
ya maandishi hayo, iliyopaswa
kutolewa iwe sheria[e] katika wi-
laya zote mbalimbali za utawa-
la[f] ilikuwa ikitangaziwa viku-
ndi vyote vya watu, ili wawe
tayari kwa siku hiyo. **15** Wa-
jumbe hao wakaondoka, wa-
kaenda haraka[g] kwa sababu
ya neno la mfalme, na sheria
hiyo ikatolewa katika ngome
ya Shushani.[h] Naye mfalme pa-
moja na Hamani wakaketi ili
kunywa;[i] bali jiji la Shushani[j] li-
kavurugika.[k]

4 Basi Mordekai[l] akapata ku-
jua mambo yote yaliyoku-
wa yamefanywa;[m] ndipo Mor-
dekai akararua mavazi yake
na kuvaa nguo za magunia[n] na
majivu,[o] akaenda katikati ya
jiji, akalia kwa sauti kubwa na
yenye uchungu.[p] **2** Mwisho-
we akaja mpaka mbele ya lango
la mfalme,[q] kwa maana haku-
na yeyote aliyepaswa kuingia
katika lango la mfalme aki-
wa amevaa nguo za magu-
nia. **3** Na katika wilaya zote
mbalimbali za utawala,[r] koko-
te ambako neno la mfalme na
sheria yake ilikuwa ikifika, ku-
litokea maombolezo[s] makubwa
kati ya Wayahudi, na kufu-
nga,[t] na kulia, na kuomboleza.
Na wengi wakatandika nguo
za magunia[u] na majivu[v] kuwa
vitanda vyao. **4** Na wanawa-
ke vijana wa Esta na matowa-
shi[a] wake wakaingia na kumpa
habari. Na malkia akaumia
sana. Kisha akaagiza mavazi
ya kumvika Mordekai yapele-
kwe na nguo zake za magu-
nia zivuliwe. Naye hakuyaku-
bali.[b] **5** Kisha Esta akamwita
Hathaki,[c] mmoja wa matowa-
shi wa mfalme, ambaye mfa-
lme alikuwa amemweka amhu-
dumie Esta, akampa amri ku-
mhusu Mordekai, apate kuya-
jua mambo hayo na maana
yake.

6 Basi Hathaki akaenda
kwa Mordekai kwenye kiwanja
cha watu wote cha jiji kilicho-
kuwa mbele ya lango la mfa-
lme. **7** Ndipo Mordekai aka-
mweleza kuhusu mambo yote
yaliyompata[d] na taarifa kamili
ya pesa ambazo Hamani aliku-
wa amesema atalipa kwa hazi-
na[e] ya mfalme juu ya Wayahu-
di, ili kuwaangamiza.[f] **8** Naye
akampa nakala[g] ya maandishi
ya sheria ya kuwaangamiza ili-
yokuwa imetolewa Shushani[h]
ili amwonyeshe Esta na ku-
mweleza na kumwagiza[i] kwa-
mba aingie kwa mfalme na
kumwomba kibali[j] na kutoa
ombi moja kwa moja mbele
yake kwa ajili ya watu wake
mwenyewe.[k]

9 Basi Hathaki[l] akaingia na
kumwambia Esta maneno
ya Mordekai. **10** Ndipo Esta
akamwambia Hathaki na ku-
mwamuru hivi kumhusu Mor-
dekai:[m] **11** "Watumishi wote
wa mfalme na watu wa wila-
ya za utawala wa mfalme wa-
najua kwamba mwanamume
au mwanamke yeyote anaye-
ingia kwa mfalme katika ua
wa ndani[n] bila kuitwa, mfa-
lme ana sheria moja tu,[o] kwa-
mba mtu huyo auawe; ila tu

SURA 3
a 2Nya 30:6, Est 8:14, Yer 51:31
b Est 8:12
c Est 9:1
d Est 8:11, Est 9:10
e Da 6:15
f Est 1:1
g Est 8:14
h Da 8:2
i Met 31:4
j Est 4:16
k Met 29:2

SURA 4
l Est 2:5
m Est 3:8, Est 3:9
n 1Fa 21:27, Zb 69:11, Ufu 6:12
o Eze 27:30, Mt 11:21
p Eze 21:6, Mik 1:8
q Est 6:10
r Est 1:1
s Yer 6:26, Amo 5:16
t 2Nya 20:3, Ezr 8:21, Mt 4:2
u 2Sa 21:10, Isa 58:5
v Eze 27:30, Da 9:3

Safu ya 2
a Est 2:3, Est 2:14
b Zb 77:2
c Est 4:10
d Est 3:8
e Est 3:9
f Est 3:13
g Est 3:14
h Est 3:15
i Est 2:20
j Met 16:15, Mhu 10:4
k Est 7:3
l Est 4:5
m Est 2:5, Est 2:7
n Est 5:1
o Da 6:15

mfalme akimnyooshea fimbo
yake ya enzi ya dhahabu, ndipo
atakapoendelea kuishi.[a] Lakini
mimi, kwa siku 30 sasa sijaitwa
kuingia kwa mfalme."
12 Nao wakamwambia Mordekai maneno ya Esta. **13** Ndipo Mordekai akasema Esta apewe jibu hili: "Usiwaze katika nafsi yako mwenyewe kwamba nyumba ya mfalme itaponyoka kuliko Wayahudi wengine wote.[b] **14** Kwa maana ukinyamaza kabisa wakati huu, msaada na ukombozi wa Wayahudi utasimama kutoka mahali pengine;[c] bali wewe pamoja na nyumba ya baba yako, mtaangamizwa. Na ni nani anayejua ikiwa si kwa ajili ya wakati kama huu kwamba umefikia heshima ya kifalme?"[d]

15 Basi Esta akasema Mordekai apewe jibu la kusema: **16** "Nenda, wakusanye Wayahudi wote waliopo Shushani[e] na mfunge[f] kwa ajili yangu, msile wala kunywa kwa siku tatu,[g] usiku na mchana. Mimi pia pamoja na wanawake wangu vijana,[h] nitafunga vivyo hivyo, na baada ya hapo nitaingia kwa mfalme, jambo ambalo ni kinyume cha sheria. Nami nikiangamia,[i] na niangamie." **17** Kwa hiyo Mordekai akaenda zake na kufanya kulingana na yote ambayo Esta alikuwa amemwamuru.

5 Na ikawa kwamba siku ya tatu[j] Esta akavaa mavazi ya kifalme,[k] kisha akasimama katika ua wa ndani[l] wa nyumba ya mfalme kuelekeana na nyumba ya mfalme, mfalme akiwa ameketi katika kiti chake cha ufalme ndani ya nyumba ya kifalme kuelekeana na lango la nyumba. **2** Na ikawa kwamba, mara tu mfalme alipomwona Malkia Esta amesimama katika ua, akapata kibali[a] machoni pake, naye mfalme akamnyooshea Esta fimbo yake ya enzi ya dhahabu[b] iliyokuwa mkononi mwake. Basi Esta akakaribia na kuigusa ncha ya fimbo hiyo ya enzi.

3 Ndipo mfalme akamwambia: "Una nini, Ee Esta, malkia, na ombi lako ni nini?[c] Hata nusu ya ufalme[d]—na upewe wewe!" **4** Naye Esta akasema: "Mfalme akiona vema, mfalme na aje leo pamoja na Hamani[e] kwenye karamu[f] ambayo nimemwandalia." **5** Basi mfalme akasema: "Ninyi watu, mwambieni Hamani afanye haraka[g] kulingana na neno la Esta." Baadaye mfalme na Hamani wakaja kwenye karamu ambayo Esta alikuwa ameandaa.

6 Baada ya muda mfalme akamwambia Esta wakati wa karamu ya divai: "Ombi lako ni nini?[h] Na upewe hilo! Hata nusu ya ufalme—na upewe wewe!" **7** Kwa hiyo Esta akajibu, akasema: "Haja yangu na ombi langu ni hili, **8** Ikiwa nimepata kibali machoni pa mfalme,[i] na ikiwa inaonekana vema kwa mfalme kunipa haja yangu na kufanya kulingana na ombi langu, mfalme pamoja na Hamani na waje kwenye karamu ambayo nitawafanyia kesho, nami kesho nitafanya kulingana na neno la mfalme."[j]

9 Basi Hamani akatoka siku hiyo akiwa na shangwe na furaha[k] moyoni; lakini mara tu Hamani alipomwona Mordekai katika lango la mfalme[l]

SURA 4
a Est 5:2
Est 8:4
b Met 24:10
Met 29:25
Yoh 12:25
c 1Sa 12:22
Isa 54:17
Yer 30:11
Amo 9:8
d Zb 75:7
Isa 14:27
Isa 49:23
e Est 3:15
f 2Nya 20:3
Ezr 8:21
Mt 4:2
g Est 5:1
h Est 2:9
i Zb 34:15
Zb 55:22
Zb 62:8
Zb 115:9
Met 29:25
Ro 16:4

SURA 5
j Est 4:16
k Est 2:17
Est 8:15
Mt 11:8
l Est 4:11
Est 6:4

Safu ya 2
a Zb 116:7
b Est 4:11
Est 8:4
c Est 7:2
Est 9:12
d Mk 6:23
e Est 3:1
Est 3:8
f Mwa 32:20
Met 17:8
g Est 6:14
h Est 7:2
i Est 5:3
j Met 29:11
k Ayu 20:5
Lu 6:25
Yak 4:9
l Est 2:21
Est 3:3
Est 6:10

na kwamba hakusimama[a] wala
kutetemeka kwa ajili yake,[b]
upesi Hamani akajawa na
ghadhabu[c] juu ya Mordekai.
10 Hata hivyo, Hamani aka-
jizuia na kwenda nyumbani
kwake. Kisha akatuma neno
ili rafiki zake na Zereshi[d] mke
wake waletwe; **11** naye Ha-
mani akawatangazia utuku-
fu wa utajiri[e] wake na hesa-
bu kubwa ya wanawe[f] na kila
kitu ambacho mfalme aliku-
wa amemtukuza nacho na ji-
nsi alivyokuwa amemwinua
juu ya wakuu na watumishi wa
mfalme.[g]

12 Tena Hamani akasema:
"Zaidi ya hayo, Esta, malkia,
hakumkaribisha mtu yeyote
pamoja na mfalme kwenye ka-
ramu isipokuwa mimi,[h] na ke-
sho[i] pia nimealikwa naye pamo-
ja na mfalme. **13** Lakini hayo
yote hayana faida yoyote kwa-
ngu ninapomwona yule Mor-
dekai Myahudi ameketi kati-
ka lango la mfalme." **14** Ndi-
po Zereshi mke wake na rafiki
zake wote wakamwambia: "Na
watengeneze mti[j] wenye ure-
fu wa mikono 50. Kisha asu-
buhi[k] umwambie mfalme kwa-
mba wamtundike Mordekai juu
yake.[l] Halafu uingie pamoja na
mfalme kwenye karamu ukiwa
na shangwe." Basi jambo
hilo likaonekana jema[m] mbele
ya Hamani, naye akautengeneza
mti.[n]

6 Usiku huo usingizi wa mfa-
lme ulimtoka.[o] Kwa hiyo
akasema kwamba kitabu cha
kumbukumbu[p] za mambo ya
nyakati kiletwe. Kisha mambo
hayo yakasomwa mbele ya mfa-
lme. **2** Mwishowe wakapata
maandishi ya habari ambazo
Mordekai alikuwa ametoa[q] juu
ya Bigthana na Tereshi, mao-
fisa wawili[a] wa makao ya mfa-
lme, watunza-milango, walio-
kuwa wametafuta kunyoosha
mkono juu ya Mfalme Ahasue-
ro. **3** Ndipo mfalme akasema:
"Mordekai amefanyiwa heshi-
ma na jambo gani kubwa kwa
ajili ya hayo?" Nao watumishi
wa mfalme, wahudumu wake,
wakasema: "Hajafanyiwa lo-
lote."[b]

4 Baadaye mfalme akasema:
"Ni nani aliye katika ua?" Basi
Hamani alikuwa amekuja kati-
ka ua wa nje[c] wa nyumba ya
mfalme ili kumwambia mfa-
lme kwamba Mordekai atundi-
kwe juu ya mti[d] ambao alikuwa
amemwekea tayari. **5** Nao
watumishi wa mfalme waka-
mwambia: "Tazama, Hamani[e]
anasimama katika ua." Kisha
mfalme akasema: "Mwacheni
aingie."

6 Hamani alipoingia, mfa-
lme akamwambia: "Mtu amba-
ye mfalme amependa kumhe-
shimu afanyiwe nini?" Ndipo
Hamani akasema moyoni mwa-
ke:[f] "Mfalme angependa ku-
mheshimu nani kuliko mimi?"[g]
7 Kwa hiyo Hamani akamwa-
mbia mfalme: "Kuhusu mtu
ambaye mfalme amependa ku-
mheshimu, **8** na walete ma-
vazi ya kifalme[h] ambayo mfa-
lme huvaa na farasi ambaye
mfalme hupanda[i] ambaye ame-
vikwa taji la kifalme juu ya ki-
chwa chake. **9** Na mmoja wa
wakuu wenye cheo[j] wa mfalme
apewe yale mavazi na yule fa-
rasi; nao wamvike mtu amba-
ye mfalme amependa kumhe-
shimu, nao wampandishe juu
ya farasi katika kiwanja cha
watu wote[k] cha jiji,[l] nao wa-
paaze sauti mbele yake, 'Hivi

SURA 5
a Est 3:2
b Zb 27:3
Zb 139:21
Zb 139:22
Mt 10:28
c Est 3:5
Mhu 7:9
d Est 5:14
Est 6:13
e Ayu 31:24
Zb 49:6
Zb 49:17
Yer 9:23
Mt 23:12
1Ti 6:17
f Est 9:10
Ayu 27:14
g Est 3:1
Zb 37:35
h Est 5:5
i Est 5:8
j Kum 21:22
Est 2:23
Est 7:9
k Met 27:1
l Est 3:2
Est 6:4
m Met 29:12
n Zb 37:14
Met 1:18
Met 21:24
Met 27:4

SURA 6
o Met 21:1
Da 2:1
Da 6:18
p Est 10:2
q Est 2:23
Est 7:9

Safu ya 2
a Est 2:21
b Met 3:27
Mhu 9:15
c Est 4:11
Est 5:1
d Est 5:14
Est 7:9
e Est 3:1
f Met 14:35
Met 16:15
Met 19:12
g Est 3:2
Est 5:11
Met 16:18
Met 18:12
Met 30:13
h Est 8:15
i 1Fa 1:38
j Est 1:3
Est 1:14
Est 3:1
k Est 4:6
l Est 3:15

ndivyo anavyofanyiwa mtu
ambaye mfalme amependa ku-
mheshimu.'"[a] **10** Mara moja
mfalme akamwambia Hamani:
"Fanya haraka, chukua mava-
zi na farasi, kama ulivyosema,
umfanyie hivyo Mordekai yule
Myahudi anayeketi katika la-
ngo la mfalme. Usiache jambo
lolote likose kutimia kati ya
mambo yote uliyoyasema."[b]
11 Ndipo Hamani akachu-
kua mavazi[c] na farasi, akamvi-
ka Mordekai[d] na kumpandisha
juu ya farasi kupitia katika ki-
wanja cha watu wote[e] cha jiji
na kupaaza sauti mbele yake:[f]
"Hivi ndivyo anavyofanyiwa
mtu ambaye mfalme amependa
kumheshimu."[g] **12** Baadaye
Mordekai akarudi kwenye la-
ngo la mfalme.[h] Lakini Hamani
akafanya haraka kwenda nyu-
mbani kwake akiomboleza, na
kichwa chake kikiwa kimefuni-
kwa.[i] **13** Halafu Hamani aka-
msimulia Zereshi[j] mke wake na
rafiki zake wote juu ya mambo
yote yaliyompata. Ndipo watu
wake wenye hekima[k] na Zere-
shi mke wake wakamwambia:
"Ikiwa Mordekai, ambaye ume-
anza kuanguka mbele yake,
anatoka katika uzao wa Waya-
hudi, wewe hutamshinda, bali
bila shaka utaanguka mbele
yake."[l]
14 Walipokuwa bado wana-
sema naye, maofisa wa makao
ya mfalme wakafika nao wa-
kafanya haraka[m] kumleta Ha-
mani kwenye karamu[n] ambayo
Esta alikuwa ameandaa.

7 Ndipo mfalme na Hama-
ni[o] wakaingia ili kula ka-
ramu pamoja na Malkia Esta.
2 Basi mfalme akamwambia
Esta siku ya pili pia wakati
wa karamu ya divai:[p] "Ombi
lako ni nini,[a] Ee Esta, malkia?
Na upewe hilo.[b] Na haja yako ni
nini? Hata nusu ya ufalme[c]—na
iwe hivyo!" **3** Kwa hiyo Esta,
malkia, akajibu, akasema: "Iki-
wa nimepata kibali machoni
pako, Ee mfalme, na mfalme
akiona vema, na nipewe nafsi[d]
yangu mwenyewe kuwa ombi
langu na watu wangu[e] kuwa
haja yangu. **4** Kwa maana tu-
meuzwa,[f] mimi na watu wangu,
tuangamizwe, tuuawe na ku-
haribiwa.[g] Basi ikiwa tungaliu-
zwa tuwe watumwa[h] na waja-
kazi, ningalinyamaza kimya.
Lakini taabu hii haifai ikiwa
inamletea mfalme hasara."
5 Sasa Mfalme Ahasuero
akasema, ndiyo, akamwambia
Malkia Esta: "Ni nani huyo,[i] na
yuko wapi mtu huyo ambaye
amejipatia ujasiri[j] wa kufanya
hivyo?" **6** Ndipo Esta akase-
ma: "Mtu huyo, mpinzani[k] na
adui,[l] ni huyu Hamani mtu
mbaya."
Basi Hamani akaogopa
sana[m] kwa sababu ya mfalme
na malkia. **7** Mfalme naye
akasimama akiwa na ghadha-
bu[n] akatoka kwenye karamu
ya divai na kwenda katika bu-
stani ya jumba la mfalme; Ha-
mani naye akasimama kutoa
ombi kwa Malkia Esta kwa aji-
li ya nafsi yake,[o] maana ali-
ona kuwa mfalme[p] ameazimia
mabaya[q] juu yake. **8** Kisha
mfalme akarudi kutoka katika
bustani ya jumba la mfa-
lme na kuingia katika nyu-
mba ya karamu ya divai;[r]
naye Hamani alikuwa amea-
ngukia kitanda[s] alipokuwa-
po Esta. Basi mfalme akasema:
"Je, malkia alalwe kinguvu vi-
levile, nami nimo nyumbani?"
Neno hilo lilitoka kinywani

SURA 6
a Mwa 41:43
2Sa 15:1
b Da 4:37
Lu 14:11
c Est 8:15
d Est 2:5
e Est 4:6
f Lu 1:52
g Est 6:6
h Est 2:21
Zb 131:1
i Zb 44:7
j Est 5:10
k Mwa 41:8
l Kum 32:35
Met 28:18
Ho 14:9
m Est 5:5
n Est 5:8

SURA 7
o Est 3:1
Est 5:12
p Est 5:6

Safu ya 2
a Est 5:3
b Est 9:12
c Mk 6:23
d Mwa 2:7
1Ko 15:45
e Est 2:7
Est 4:8
f Est 3:9
Est 4:7
Est 4:8
g Est 3:13
Est 8:11
h Mwa 37:27
Ne 5:5
Yoe 3:6
i Met 25:5
Isa 13:11
j Mdo 5:3
k Efe 6:12
l 1Sa 24:13
Zb 27:2
Mhu 5:8
m Da 5:6
n Met 14:35
Met 16:14
o Met 14:19
p Met 19:12
q 1Sa 20:9
1Sa 25:17
Zb 112:10
r Est 7:1
s Est 1:6
Mt 26:20

mwa mfalme,[a] nao wakaufunika uso wa Hamani. **9** Sasa Harbona,[b] mmoja wa maofisa wa makao ya mfalme[c] aliyetumikia mbele ya mfalme, akasema: "Pia, kuna mti[d] wenye urefu wa mikono 50 ambao Hamani aliutengeneza kwa ajili ya Mordekai, aliyesema mema kumhusu mfalme,[e] umesimama katika nyumba ya Hamani." Basi mfalme akasema: "Mtundikeni juu yake."[f] **10** Nao wakamtundika Hamani juu ya mti[g] ambao alikuwa ameweka tayari kwa ajili ya Mordekai;[h] nayo ghadhabu ya mfalme ikapungua.

8 Siku hiyo Mfalme Ahasuero alimpa Esta, malkia, nyumba ya Hamani,[i] ambaye aliwaonyesha Wayahudi uadui;[j] naye Mordekai akaingia mbele ya mfalme, kwa maana Esta alikuwa amesema yeye ni nani kwake.[k] **2** Kisha mfalme akavua pete yake ya muhuri[l] aliyokuwa amempokonya Hamani, akampa Mordekai; naye Esta akamweka Mordekai juu ya nyumba ya Hamani.[m]

3 Tena, Esta akasema mara nyingine mbele ya mfalme na kuanguka chini miguuni pake, akalia na kumwomba[n] kibali augeuzie mbali ubaya[o] wa Hamani Mwagagi na hila[p] yake aliyokuwa amepanga juu ya Wayahudi.[q] **4** Ndipo mfalme akamnyooshea Esta fimbo ya enzi ya dhahabu,[r] basi Esta akainuka na kusimama mbele ya mfalme. **5** Sasa akasema: "Ikiwa inaonekana vema kwa mfalme, na ikiwa nimepata kibali[s] mbele yake na jambo hili linafaa mbele ya mfalme nami ni mwema machoni pake, na iandikwe kwamba zile barua zifutwe,[a] ule mpango wa hila wa Hamani mwana wa Hamedatha Mwagagi,[b] ambazo aliandika kuwaangamiza Wayahudi[c] walio katika wilaya zote za utawala[d] wa mfalme. **6** Kwa maana ninawezaje kuvumilia kutazama msiba utakaowapata watu wangu, nami ninawezaje kuvumilia kutazama maangamizi ya jamaa zangu?"

7 Basi Mfalme Ahasuero akamwambia Malkia Esta na Mordekai Myahudi: "Tazama! Nimempa Esta[e] nyumba ya Hamani, naye wamemtundika mtini,[f] kwa sababu alinyoosha mkono wake juu ya Wayahudi. **8** Nanyi andikeni kwa ajili ya Wayahudi kulingana na yaliyo mema machoni penu wenyewe katika jina la mfalme,[g] nanyi myatie muhuri kwa pete ya mfalme; kwa maana maandishi ambayo yameandikwa kwa jina la mfalme na kutiwa muhuri kwa pete ya mfalme hayawezi kufutwa."[h]

9 Basi waandishi[i] wa mfalme wakaitwa wakati huo katika mwezi wa tatu, yaani, mwezi wa Sivani, siku ya 23 ya mwezi huo; na Wayahudi na maliwali[j] na magavana na wakuu wa wilaya za utawala ambazo zilikuwa kutoka India mpaka Ethiopia, wilaya za utawala 127,[k] wakaandikiwa kulingana na yote ambayo Mordekai aliamuru. Kila wilaya ya utawala kwa mtindo wao wa kuandika[l] na kila kikundi cha watu kwa lugha[m] yao, na Wayahudi kwa mtindo wao wa kuandika na kwa lugha[n] yao.

10 Naye akaandika kwa jina la Mfalme[o] Ahasuero na kutia muhuri[p] kwa pete ya mfalme[q]

SURA 7

a Met 16:14
b Est 1:10
c Mwa 37:36; Est 2:21
d Est 5:14
e Est 6:2
f Zb 7:6; Zb 9:15; Zb 35:8; Zb 73:19; Met 11:6
g Est 5:14
h Zb 37:34; Met 21:18; 2Pe 2:9

SURA 8

i Est 5:11
j Est 3:8; Est 9:24
k Est 2:5; Est 2:7
l Mwa 41:42; Est 3:10; Da 6:17
m Mhu 2:18; Da 2:48
n Ho 12:4; Lu 11:9
o Est 3:9
p Est 9:25
q Est 7:4; Est 9:24
r Est 4:11
s Est 2:17

Safu ya 2

a Est 3:12; Est 3:14
b Hes 24:7; Kum 25:19; 1Sa 15:8; Est 9:24
c Est 3:9
d Est 1:1
e Est 8:1; Met 13:22
f Est 7:10; Ga 3:13
g 1Fa 21:8; Est 3:12
h Da 6:8; Da 6:15
i Est 3:12
j Ezr 8:36; Est 9:3; Da 6:1
k Est 1:1
l Est 1:22; Est 3:12
m Da 4:1
n 1Ko 14:9
o Mhu 8:4
p Est 3:12
q Est 8:2

na kupeleka barua kwa mkono wa wajumbe waliopanda farasi[a] wenye kusafirisha barua wanaotumiwa katika utumishi wa kifalme, wana-farasi wenye mbio, **11** kwamba mfalme alitoa ruhusa kwa Wayahudi walio katika majiji yote mbalimbali wajikusanye[b] na kusimama kwa ajili ya nafsi zao, waangamize, waue, na kuharibu jeshi lote la watu[c] na wilaya za utawala zilizokuwa zikiwaonyesha uadui, watoto kwa wanawake, na kupora nyara zao,[d] **12** siku moja[e] katika wilaya zote za utawala za Mfalme Ahasuero, siku ya kumi na tatu[f] ya mwezi wa kumi na mbili, yaani, mwezi wa Adari.[g] **13** Nakala[h] ya maandishi hayo ingetolewa kama sheria katika wilaya zote mbalimbali za utawala, ikitangaza kwa vikundi vyote vya watu, kwamba Wayahudi walipaswa kuwa tayari kwa ajili ya siku hiyo ili wajilipizie kisasi[i] juu ya adui zao. **14** Wajumbe[j] nao, wakiwa wamepanda farasi wenye kusafirisha barua wanaotumiwa katika utumishi wa kifalme, wakaondoka, wakiwa wanachochewa kwenda mbele na kuendeshwa mbio[k] kwa sababu ya neno la mfalme; na sheria hiyo ilitolewa katika ngome ya Shushani.[l]

15 Naye Mordekai akatoka mbele ya mfalme akiwa amevaa mavazi ya kifalme[m] ya bluu na kitani, taji kubwa la dhahabu, na kanzu ya kitambaa laini,[n] ya sufu iliyotiwa rangi ya zambarau.[o] Na jiji la Shushani likapaaza sauti na kushangilia.[p] **16** Kwa Wayahudi kukawa nuru na kushangilia[q] na furaha na heshima. **17** Na katika wilaya zote mbalimbali za utawala na katika majiji yote mbalimbali ambako neno la mfalme na sheria yake ilifika kulikuwa na shangwe na furaha kwa Wayahudi, karamu[a] na siku njema; na watu wengi[b] wa nchi wakawa wanajitangaza wenyewe kuwa Wayahudi,[c] maana hofu[d] ya Wayahudi ilikuwa imewashika.

9 Na katika mwezi wa kumi na mbili, yaani, mwezi wa Adari,[e] siku ya kumi na tatu ya mwezi huo, wakati ulipofika wa kutimiza neno la mfalme na sheria yake,[f] siku ambayo adui za Wayahudi walikuwa wamengojea kuwatawala, mambo yaligeuka yakawa kinyume, kwa maana Wayahudi waliwatawala wale waliowachukia.[g] **2** Wayahudi walijikusanya[h] katika majiji yao katika wilaya zote za utawala wa Mfalme Ahasuero[i] ili kunyoosha mikono yao juu ya wale waliotafuta kuwaumiza,[j] wala hakuna hata mtu mmoja aliyeweza kusimama mbele yao, kwa maana vikundi vyote vya watu walikuwa wameshikwa na hofu[k] kwa sababu yao. **3** Na wakuu wote[l] wa wilaya za utawala na maliwali[m] na magavana na watendaji wa kazi[n] za mfalme walikuwa wakiwasaidia Wayahudi, kwa maana walikuwa wameshikwa na hofu[o] kwa sababu ya Mordekai. **4** Kwa maana Mordekai alikuwa mkuu[p] katika nyumba ya mfalme na sifa yake[q] ilivuma kotekote katika wilaya zote za utawala, kwa sababu huyo Mordekai alikuwa akizidi kuwa mkuu.[r]

5 Nao Wayahudi wakawapiga adui zao wote kwa maua-

SURA 8
a Est 3:13
b Est 9:2
c Zb 37:14
Zb 68:2
d Est 3:13
Est 9:10
Est 9:15
Est 9:16
e Kut 15:9
f Est 3:13
Est 9:1
g Est 9:17
Est 9:21
h Est 3:14
i Zb 92:11
Zb 149:7
Lu 18:7
j Est 3:13
k Est 3:15
l Est 1:2
Da 8:2
m Mwa 41:42
Est 6:8
Lu 16:19
n Mt 11:8
o Kut 25:4
Kut 28:5
p Met 29:2
q Est 9:17
Zb 18:28
Zb 30:5
Zb 97:11
Met 11:10
Isa 30:26
Mik 7:8

Safu ya 2
a Ne 8:10
Est 9:19
Est 9:22
b Zb 18:43
c Zek 8:23
d Est 9:2

SURA 9
e Est 3:7
Est 8:12
f Est 3:13
g Kum 32:36
2Sa 22:41
Zb 30:11
h Est 8:11
i Est 1:1
j Zb 71:13
Zb 71:24
k Kum 11:25
Est 8:17
l Est 3:12
Est 8:9
m Da 6:1
n Est 3:9
o Est 9:1
Zb 31:11
p Est 8:15
q 1Sa 2:30
Sef 3:19
r 2Nya 1:1
Zb 1:3

ji ya upanga,[a] wakawaua na
kuwaangamiza, nao wakawate-
ndea walivyotaka wale walio-
wachukia.[b] **6** Na katika ngo-
me ya Shushani[c] Wayahudi wa-
liwaua na kuwaangamiza watu
mia tano. **7** Pia, Parshan-
datha na Dalfoni na Aspa-
tha **8** na Poratha na Adalia
na Aridatha **9** na Parmashta
na Arisai na Aridai na Vai-
zatha, **10** wana kumi[d] wa Ha-
mani[e] mwana wa Hamedatha,
yule aliyewaonyesha Wayahu-
di uadui,[f] wakawaua hao; laki-
ni hawakunyoosha mkono wao
juu ya nyara.[g]

11 Siku hiyo hesabu ya wa-
liouawa katika ngome ya Shu-
shani ikaletwa mbele ya mfa-
lme.

12 Na mfalme akamwambia
Malkia Esta:[h] "Katika ngome[i]
ya Shushani Wayahudi wame-
waua na kuwaangamiza watu
mia tano pamoja na wana kumi
wa Hamani. Katika wilaya nyi-
nginezo za utawala[j] wa mfa-
lme wamefanya nini?[k] Na ombi
lako ni nini? Na upewe hilo.[l]
Na haja yako zaidi ni nini?[m]
Na ifanywe." **13** Kwa hiyo
Esta akasema: "Ikiwa kwa mfa-
lme inaonekana vema,[n] Waya-
hudi walio katika Shushani na
wapewe ruhusa kesho pia ku-
fanya kulingana na sheria ya
leo;[o] na hao wana kumi wa Ha-
mani watundikwe juu ya mti."[p]
14 Basi mfalme akasema ifa-
nywe hivyo.[q] Ndipo sheria ika-
tolewa katika Shushani, na
wale wana kumi wa Hamani
wakatundikwa mtini.

15 Na Wayahudi waliokuwa
Shushani wakajikusanya pia
siku ya kumi na nne[r] ya mwezi
wa Adari, nao wakawaua watu
mia tatu Shushani; lakini ha-
wakunyoosha mkono wao juu
ya nyara.[a]

16 Na wale Wayahudi wengi-
ne waliokuwa katika wilaya za
utawala[b] wa mfalme, walijiku-
sanya, wakasimama kwa ajili
ya nafsi[c] zao, wakajilipizia ki-
sasi[d] juu ya adui zao na kuua
watu 75,000 kati ya wale wali-
owachukia; lakini hawakunyo-
osha mkono wao juu ya nya-
ra, **17** katika siku ya kumi na
tatu ya mwezi wa Adari; na ku-
kawa na pumziko siku ya kumi
na nne ya mwezi huo, nayo ika-
fanywa kuwa siku ya karamu[e]
na kushangilia.[f]

18 Nao Wayahudi walioku-
wa Shushani, wakajikusanya
siku ya kumi na tatu[g] na siku
ya kumi na nne ya mwezi huo,
kukawa na pumziko siku ya
kumi na tano ya mwezi huo,
nayo ikafanywa kuwa siku
ya karamu na kushangilia.[h]
19 Ndiyo sababu Wayahudi wa
mashambani, waliokaa katika
majiji ya wilaya za utawala zi-
lizo kandokando, walikuwa wa-
kiifanya siku ya kumi na nne
ya mwezi wa Adari[i] kuwa siku
ya kushangilia,[j] ya karamu na
siku njema[k] na ya kupelekeana
mafungu[l] ya vitu.

20 Naye Mordekai[m] akaa-
ndika mambo hayo na kuagi-
za barua zipelekwe kwa Wa-
yahudi wote waliokuwa kati-
ka wilaya zote za utawala[n] wa
Mfalme Ahasuero, zilizo karibu
na zilizo mbali pia, **21** kuwa-
wekea wajibu[o] wawe wakishi-
ka kwa ukawaida siku ya kumi
na nne ya mwezi wa Adari na
siku ya kumi na tano ya mwe-
zi huo mwaka baada ya mwaka,
22 kulingana na siku ambazo
Wayahudi walipumzika kuto-
kana na adui[p] zao na mwezi

SURA 9

a Zb 18:34
Zb 18:47
Mik 5:8
2Th 1:6
b 1Sa 12:22
Zb 34:19
Zb 94:14
Mik 5:9
c Est 1:2
Da 8:2
d Kut 17:14
Kut 17:16
Hes 24:7
Zb 21:10
Zb 109:13
e Est 3:1
Est 3:12
Est 8:5
f Est 3:8
Est 7:4
g Est 8:11
Est 9:16
h Est 2:17
i Est 3:15
j Est 1:1
Da 6:1
k Est 9:16
l Est 5:6
m Est 8:5
n Est 5:8
Est 7:3
o Est 8:11
p Kum 21:22
Est 2:23
Est 7:10
Ga 3:13
q Est 9:25
r Est 9:21
Est 9:31

Safu ya 2

a Est 9:10
b Est 1:1
Da 6:1
c Mwa 2:7
Law 17:11
Est 7:3
d Kum 32:35
Est 8:13
Zb 149:7
Nah 1:2
Lu 18:7
e Est 8:17
f Est 8:16
Zb 58:10
g Est 9:1
Est 9:13
Est 9:15
h Met 11:10
i Ezr 6:15
Est 3:7
j Zb 118:15
Zb 145:7
Isa 65:14
k Zb 124:2
Zb 124:6
l Ne 8:10
m Est 2:5
Est 8:8
n Est 1:1
Da 6:1
o Zb 145:4
p Zb 103:2
Isa 12:1

ambao huzuni yao iligeuzwa
kuwa shangwe na maombolezo[a] yakawa siku njema, wazi-
shike ziwe siku za karamu na
kushangilia na kupelekeana
mafungu[b] ya vitu na zawadi
kwa maskini.[c]
23 Nao Wayahudi wakaku-
bali mambo ambayo walikuwa
wameanza kufanya na
yale ambayo Mordekai alikuwa
amewaandikia. **24** Kwa maa-
na Hamani[d] mwana wa Hame-
datha[e] Mwagagi,[f] yule aliye-
waonyesha Wayahudi wote ua-
dui,[g] alikuwa amepanga hila
juu ya Wayahudi ili kuwaa-
ngamiza,[h] naye alikuwa ame-
fanya Puri,[i] yaani, Kura,[j] ipi-
gwe, ili kuwahangaisha na ku-
waangamiza. **25** Lakini mfa-
lme alisema kwa barua wakati
Esta alipoingia mbele yake:[k]
"Hila[l] mbaya ambayo amepa-
nga juu ya Wayahudi na irudi
juu ya kichwa chake mwenye-
we";[m] nao wakamtundika pa-
moja na wanawe juu ya mti.[n]
26 Ndiyo sababu waliziita siku
hizo Purimu, kufuatia jina la
Puri.[o] Ndiyo sababu, kulingana
na maneno yote ya barua hii[p]
na yote ambayo walikuwa wa-
meona kuhusiana na hayo na
yale ambayo yalikuwa yame-
wafikia, **27** Wayahudi, uzao
wao, na wale wote waliojiu-
nga nao,[q] walijiwekea wajibu
na kukubali kwamba usipiti-
lie mbali wajibu wa kuzishika
kwa ukawaida siku hizo mbi-
li kulingana na mambo yali-
yoandikwa kuwahusu na kuli-
ngana na wakati wake uliowe-
kwa mwaka baada ya mwaka.
28 Na siku hizo zilipasa kuku-
mbukwa na kushikwa na kiza-
zi baada ya kizazi, kila fami-
lia, kila wilaya ya utawala na
kila jiji, na siku hizo za Purimu
zisipitilie mbali kutoka katika-
ti ya Wayahudi wala ukumbu-
sho[a] wake usikome kati ya uzao
wao.
29 Na Malkia Esta, binti ya
Abihaili,[b] na Mordekai Myahu-
di, wakaandika kwa mamlaka
yote ili kuthibitisha barua
hii ya pili iliyohusu Purimu.
30 Kisha akatuma barua kwa
Wayahudi wote katika zile wi-
laya 127, za utawala[c] wa Ahasu-
ero,[d] katika maneno ya amani
na kweli,[e] **31** ili kuthibitisha
siku hizo za Purimu kwa waka-
ti wake uliowekwa, kama vile
Mordekai Myahudi, na Malkia
Esta walivyokuwa wamewa-
wekea kuwa wajibu,[f] na kama
vile walivyokuwa wamejiwe-
kea kuwa wajibu juu ya nafsi
zao wenyewe na juu ya uzao
wao,[g] mambo ya kufunga[h] na
kilio chao cha kuomba msaa-
da.[i] **32** Na neno la Esta lika-
thibitisha mambo hayo ya Puri-
mu,[j] nayo yakaandikwa katika
kitabu.

10 Naye Mfalme Ahasuero
akaweka kazi ya kulazi-
mishwa[k] juu ya nchi na visiwa[l]
vya bahari.
2 Basi kuhusu kazi zake
zote zenye nguvu na uwezo
wake na taarifa kamili ya ukuu
wa Mordekai[m] ambao mfalme
alimtukuza[n] nao, je, mambo
hayo hayakuandikwa katika
Kitabu cha mambo[o] ya nyakati
ya wafalme wa Umedi na Uaje-
mi?[p] **3** Kwa maana Mordekai
Myahudi alikuwa wa pili[q] kwa
Mfalme Ahasuero naye aliku-
wa mkuu kati ya Wayahudi na
alikubaliwa na wengi wa ndugu
zake, akifanya kazi kwa ajili ya
mema ya watu wake na kusema
amani[r] kwa uzao wao wote.

SURA 9
a Est 4:3
b Est 9:19
Lu 11:41
c Ga 2:10
d Est 3:1
e Est 8:5
f Kut 17:16
Hes 24:7
1Sa 15:8
g Est 3:10
Est 9:10
h Est 3:9
i Est 3:7
j Yoe 3:3
Oba 11
Mt 27:35
k Est 8:5
Est 8:10
Est 9:13
l Est 8:3
m Kum 19:19
Zb 7:16
Zb 37:15
Zb 141:10
Da 6:24
n Est 5:14
Est 7:10
Est 9:14
o Est 3:7
p Est 9:20
q Law 19:34
Law 24:22
Ru 1:16
1Fa 8:43
Est 8:17
Ga 5:3

Safu ya 2
a Zb 103:2
b Est 2:15
c Est 8:9
Est 9:20
d Est 1:1
e Isa 39:8
f Est 9:21
g Est 9:27
h 2Nya 20:3
Yoe 2:12
i Est 4:1
Zb 65:2
Zb 142:1
j Est 9:26

SURA 10
k Yos 16:10
Omb 1:1
l Mwa 10:5
m Est 2:5
n Est 8:15
Zb 18:35
Da 2:48
o Ezr 4:15
Est 6:1
p Est 1:3
Da 6:15
q Mwa 41:40
Da 5:16
r Zb 125:5
Met 12:20
Isa 26:12

AYUBU

1 Palikuwa na mtu katika nchi ya Usi[a] ambaye jina lake lilikuwa Ayubu;[b] na mtu huyo alikuwa asiye na lawama[c] na mnyoofu,[d] na mwenye kumwogopa Mungu[e] na kujiepusha na ubaya.[f] **2** Na wana saba na binti watatu walizaliwa kwake.[g] **3** Na mifugo[h] yake ilikuwa ni kondoo elfu saba na ngamia elfu tatu na jozi mia tano za ng'ombe na punda-jike mia tano, pamoja na kundi kubwa sana la watumishi; na mtu huyo akawa mkuu kuliko watu wote wa Mashariki.[i]

4 Na wanawe walienda na kufanya karamu[j] katika nyumba ya kila mmoja kwenye siku yake mwenyewe; nao wakatuma na kuwakaribisha dada zao watatu ili wale chakula na kunywa pamoja nao. **5** Na ilikuwa kwamba wakati siku za karamu zimemaliza mzunguko, Ayubu alikuwa akituma na kuwatakasa;[k] naye aliamka asubuhi na mapema na kutoa dhabihu za kuteketezwa[l] kulingana na hesabu yao wote; kwa kuwa Ayubu alisema, "labda wanangu wametenda dhambi nao wamemlaani[m] Mungu moyoni mwao."[n] Hivyo ndivyo Ayubu alivyofanya sikuzote.[o]

6 Na ikaja siku ambapo wana wa Mungu wa kweli[p] waliingia na kusimama mbele za Yehova,[q] na hata Shetani[r] akaingia katikati yao.[s]

7 Ndipo Yehova akamwambia Shetani: "Wewe unatoka wapi?" Naye Shetani akamjibu Yehova, akasema: "Ninatoka kuzurura huku na huku duniani[a] na kutembea huku na huku ndani yake."[b] **8** Naye Yehova akaendelea kumwambia Shetani: "Je, umeuweka moyo wako juu ya mtumishi wangu Ayubu, kwamba hakuna yeyote aliye kama yeye duniani,[c] mtu asiye na lawama[d] na mnyoofu,[e] mwenye kumwogopa Mungu[f] na kujiepusha na ubaya?"[g] **9** Ndipo Shetani akamjibu Yehova, akasema: "Je, Ayubu amemwogopa Mungu bure?[h] **10** Je, wewe hukuweka ukuta kumzunguka[i] yeye na kuzunguka nyumba yake na kuzunguka kila kitu alicho nacho pande zote? Umeibariki[j] kazi ya mikono yake, na mifugo yake imeenea kotekote duniani. **11** Lakini, ili kuwe na badiliko, tafadhali nyoosha mkono wako, uguse kila kitu alicho nacho, uone kama hatakulaani wewe mbele za uso wako."[k] **12** Basi Yehova akamwambia Shetani: "Tazama! Kila kitu alicho nacho kimo mkononi mwako. Ila tu usinyooshe mkono wako juu yake mwenyewe!" Kwa hiyo Shetani akaondoka mbele za uso wa Yehova.[l]

13 Sasa ikaja siku ambapo wanawe na binti zake walikuwa wakila na kunywa divai katika nyumba ya ndugu yao, mzaliwa wa kwanza.[m] **14** Na mjumbe[n] akamjia Ayubu na kusema: "Ng'ombe walikuwa wakilima[o] na punda-jike walikuwa wakilisha kando yao **15** ndipo Wasabea[p] wakavamia na kuwachukua, nao wakawapiga na

SURA 1

a Yer 25:20
Omb 4:21
b Eze 14:14
Eze 14:20
Yak 5:11
c Ayu 2:3
d Mwa 6:9
2Fa 20:3
e Ne 5:15
Met 8:13
Met 16:6
f 1Th 5:22
1Pe 3:11
g Zb 127:3
Zb 128:3
h 2Nya 32:29
i Mwa 29:1
1Fa 4:30
j Zb 133:1
k Kut 19:10
1Sa 16:5
l Mwa 8:20
Mwa 12:8
m Met 30:9
n Mt 15:19
o Mwa 18:19
p Mwa 6:2
Kum 33:2
Ayu 38:7
Da 3:25
q Zb 103:20
Da 7:13
Mt 18:10
r Zek 3:1
Mt 4:3
Lu 22:31
Yoh 13:2
Ufu 12:9
s 1Fa 22:19

Safu ya 2

a Ayu 2:2
b Mt 12:43
1Pe 5:8
c Hes 12:3
Met 14:35
d Mwa 6:9
Zb 37:37
Yoh 1:47
e Zb 84:11
Ebr 4:13
f Ne 5:15
Zb 19:9
Mhu 12:13
g Zb 34:14
Met 3:7
Met 16:17
h Ufu 12:10
i Mwa 15:1
Mwa 31:7
Kum 33:27
Zb 34:7
Zb 105:14
1Pe 1:5
j Mwa 26:12
Kum 28:2
Zb 5:12
Zb 84:11
Zb 128:2
Met 10:22
k Isa 8:21
l Ayu 2:7
m Ayu 1:4
n 1Sa 4:17
o 1Fa 19:19
p Ayu 6:19

kuwaua watumishi kwa makali ya upanga; nami nikaponyoka, mimi peke yangu, ili nikuambie.”[a]

16 Huyu alipokuwa bado anasema, yule naye akaja na kusema: “Moto wa Mungu ulianguka kutoka mbinguni[b] na kuwaka katikati ya kondoo na watumishi, ukawateketeza; nami nikaponyoka, mimi peke yangu, ili nikuambie.”

17 Huyu alipokuwa bado anasema, mwingine akaja na kusema: “Wakaldayo[c] walifanyiza vikosi vitatu, wakawakimbilia ngamia na kuwachukua, nao wakawapiga na kuwaua watumishi kwa makali ya upanga; nami nikaponyoka, mimi peke yangu, ili nikuambie.”

18 Huyu alipokuwa bado anasema, mwingine bado akaja na kusema: “Wana wako na binti zako walikuwa wakila na kunywa divai[d] katika nyumba ya ndugu yao, mzaliwa wa kwanza. **19** Na tazama! ukaja upepo mkubwa[e] kutoka eneo la nyikani, nao ukazipiga pembe nne za ile nyumba, hivi kwamba ikawaangukia wale vijana, nao wakafa. Nami nikaponyoka, mimi peke yangu, ili nikuambie.”

20 Naye Ayubu akasimama, akalirarua[f] koti lake lisilo na mikono, akanyoa[g] kichwa chake, akaanguka chini[h] na kuinama,[i] **21** akasema:

“Mimi nilitoka tumboni
mwa mama yangu nikiwa
uchi,[j]
Nami nitarudi huko nikiwa
uchi.[k]
Yehova ametoa,[l] na Yehova
amechukua.[m]
Jina la Yehova na liendelee
kubarikiwa.”[a]

22 Katika hayo yote Ayubu hakutenda dhambi, wala kumhesabia Mungu jambo lolote lisilofaa.[b]

2 Baadaye ikaja siku ambapo wana wa Mungu wa kweli waliingia na kusimama mbele za Yehova, na Shetani pia akaingia katikati yao na kusimama mbele za Yehova.[c]

2 Ndipo Yehova akamwambia Shetani: “Wewe unatoka wapi hasa?” Naye Shetani akamjibu Yehova, akasema: “Ninatoka kuzurura huku na huku duniani na kutembea huku na huku ndani yake.”[d] **3** Naye Yehova akaendelea kumwambia Shetani: “Je, umeweka moyo wako juu ya mtumishi wangu Ayubu,[e] kwamba hakuna yeyote aliye kama yeye duniani, mtu asiye na lawama na mnyoofu,[f] mwenye kumwogopa Mungu[g] na kujiepusha na ubaya?[h] Hata sasa bado anashikilia sana utimilifu wake,[i] ingawa wewe unanichochea[j] juu yake nimmeze bila sababu.”[k] **4** Lakini Shetani[l] akamjibu Yehova, akasema: “Ngozi kwa ngozi, na kila kitu alicho nacho mtu atakitoa kwa ajili ya nafsi yake.[m] **5** Ili kuwe na badiliko, tafadhali nyoosha mkono wako, uguse kufikia mfupa wake na nyama yake, uone kama hatakulaani wewe mbele za uso wako.”[n]

6 Basi Yehova akamwambia Shetani: “Tazama, yumo mkononi mwako! Ila tu ujihadhari na nafsi yake!” **7** Kwa hiyo Shetani akaondoka mbele za uso wa Yehova,[o] akampiga Ayubu kwa majipu[p] hatari kuanzia

SURA 1
a 1Sa 22:20
b Efe 2:2
c Mwa 11:28
2Fa 24:2
d Zb 104:15
Mhu 9:7
Mhu 10:19
e Efe 2:2
f Mwa 37:34
1Sa 4:12
g Ezr 9:3
Mik 1:16
h 2Sa 12:16
Isa 3:26
Mt 26:39
i Mwa 24:26
Kut 34:8
Ne 9:3
j Ayu 31:15
Zb 127:3
Mhu 5:15
1Ti 6:7
k Mwa 3:19
Zb 49:17
Mhu 12:7
l Mhu 5:19
Yak 1:17
m 1Sa 2:6
Met 23:5

Safu ya 2
a Zb 34:1
Da 2:20
b Kum 32:4
Ro 9:20

SURA 2
c Ayu 1:6
d Ayu 1:7
e Ayu 1:8
f Mwa 6:9
g Ne 5:15
Met 8:13
Met 16:6
h Zb 34:14
1Th 5:22
i Ayu 27:5
j Ayu 1:11
k Ayu 9:17
l Ayu 1:6
m Yer 41:8
n Law 24:15
Ayu 1:11
Ufu 12:10
o Ayu 1:12
p Kut 9:9
Law 13:18
Ayu 30:30

wayo wa mguu wake mpaka
kwenye utosi wa kichwa cha-
ke. **8** Naye akajichukulia ki-
gae cha udongo cha kujikunia;
naye akawa akiketi katikati ya
majivu.[a]
9 Mwishowe mke wake aka-
mwambia: "Je, bado unashikilia
sana utimilifu wako?[b] Mlaani
Mungu, ufe!" **10** Lakini yeye
akamwambia: "Wewe unasema
kama anavyosema mmoja wa
hao wanawake wasio na aki-
li.[c] Je, tukubali yaliyo mema tu
kutoka kwa Mungu wa kweli,
wala tusikubali pia yaliyo ma-
baya?"[d] Katika hayo yote Ayu-
bu hakutenda dhambi kwa mi-
domo yake.[e]
11 Na rafiki watatu wa Ayu-
bu wakasikia habari za msiba
huo wote uliompata, nao wa-
kaja, kila mmoja kutoka ma-
hali pake, Elifazi Mtemani[f]
na Bildadi Mshua[g] na Sofari
Mnaamathi.[h] Kwa hiyo waka-
kutana kwa mapatano[i] ili waje
kumsikitikia na kumfariji.[j]
12 Walipoinua macho yao ku-
toka mbali hawakumtambua.
Ndipo wakapaaza sauti zao,
wakalia, wakararua[k] kila mmo-
ja koti lake lisilo na mikono
na kurusha mavumbi kuelekea
mbinguni juu ya vichwa vyao.[l]
13 Nao wakaendelea kuketi[m]
chini pamoja naye siku saba,
mchana na usiku, wala hakuna
yeyote aliyemwambia neno lo-
lote, kwa maana waliona kwa-
mba yale maumivu[n] ni makali
sana.

3 Ilikuwa baada ya hayo kwa-
mba Ayubu akafungua ki-
nywa chake, akaanza kuilaa-
ni siku yake.[o] **2** Basi Ayubu
akajibu, akasema:

SURA 2
a Yer 6:26
Eze 27:30
Yon 3:6
Yon 3:8
b Mal 3:14
c Ayu 1:11
d Ayu 1:21
Yak 5:10
e Zb 39:1
Met 12:13
Yak 5:11
f Mwa 36:34
Yer 49:7
g Mwa 25:2
1Nya 1:32
h Ayu 42:9
i Amo 3:3
j Mwa 37:35
k Ayu 1:20
l Ne 9:1
Omb 2:10
Eze 27:30
m Ezr 9:3
Isa 3:26
n Ayu 16:6

SURA 3
o Yer 20:14

Safu ya 2
a Ayu 10:18
Yer 15:10
Yer 20:15
b Amo 8:10
c Ayu 10:19
d Isa 24:8
e Ayu 41:1
Ayu 41:10
Zb 74:14
Zb 104:26
f Mwa 29:31
1Sa 1:5
Ayu 10:18
g Yer 15:10
Yer 20:17

3 "Na iangamie ile siku
niliyozaliwa,[a]
Pia ule usiku ambao mtu
alisema, 'Mwanamume
amechukuliwa mimba!'
4 Siku hiyo na iwe giza.
Mungu asiiangalie kutoka
juu,
Wala nuru ya mchana
isiiangazie.
5 Giza na kivuli kizito
kiichukue.
Wingu la mvua na likae
juu yake.
Vitu vinavyotia mchana
giza na viitie hofu.[b]
6 Usiku huo—giza na
liuchukue;[c]
Usiwe na furaha katikati
ya siku za mwaka;
Usiingie katikati ya hesabu
ya miezi.
7 Tazama! Usiku huo—na
uwe tasa;
Vigelegele vyovyote vya
shangwe visije ndani
yake.[d]
8 Wenye kulaani siku na
wailaani,
Wale walio tayari
kumwamsha
Lewiathani.*[e]
9 Nyota za wakati wa
gizagiza lake na ziingiwe
na giza;
Na ungojee nuru wala
kusiwe na yoyote;
Nao usiione miali ya
mapambazuko.
10 Kwa maana haukufunga
milango ya tumbo la
uzazi la mama yangu,[f]
Na hivyo kuficha taabu
kutoka machoni pangu.
11 Kwa nini sikufa tokea
tumbo la uzazi?[g]

Ayu 3:8* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

Kwa nini sikutoka tumboni
kisha nikate pumzi?
12 Kwa nini magoti
yalinipokea,
Na kwa nini maziwa[a] ili
ninyonye?
13 Kwa maana kufikia sasa
ningalikuwa nimelala ili
nisisumbuliwe;[b]
Ningalilala wakati huo;
ningalikuwa
ninapumzika[c]
14 Pamoja na wafalme na
washauri wa dunia,[d]
Wale wanaojijengea mahali
penye ukiwa,[e]
15 Au pamoja na wakuu walio
na dhahabu,
Wale wanaozijaza nyumba
zao fedha;
16 Au, kama mimba yenye
kuharibika[f] iliyofichwa,
singalikuwako,
Kama watoto ambao
hawajaona nuru.[g]
17 Humo waovu wameacha
msukosuko,[h]
Na humo wale walioishiwa
nguvu wanapumzika.[i]
18 Wafungwa wamestarehe
pamoja;
Kwa kweli hawaisikii
sauti ya mtu
anayewalazimisha
kufanya kazi.[j]
19 Wadogo na wakubwa wamo
mle pamoja,[k]
Naye mtumwa anawekwa
huru kutoka kwa bwana
wake.
20 Kwa nini anampa nuru
yule aliye na taabu,
Na kuwapa uhai wale
wenye uchungu wa
nafsi?[l]
21 Kwa nini kuna wale
wanaongojea kifo, wala
hakipo,[m]
Ijapokuwa wanaendelea
kuchimba wakikitafuta
kuliko kutafuta hazina
zilizofichwa?
22 Wale wanaoshangilia kwa
raha,
Wanafurahi kwa sababu
wanapata kaburi.
23 Kwa nini anampa nuru
mwanamume, ambaye
njia yake imefichwa,[a]
Na ambaye Mungu
anamzungushia ukuta?[b]
24 Kwa maana kuugua
kwangu huja mbele ya
chakula changu,[c]
Na vilio vyangu vya
kunguruma[d] humwagika
kama maji;
25 Kwa sababu nimehofu kitu
chenye kutia hofu, nacho
kinakuja juu yangu;
Na kile ambacho
nimekiogopa kinanijia.[e]
26 Mimi sijawa bila
mahangaiko, wala sijawa
bila usumbufu,
Wala sijawa na pumziko,
na bado msukosuko
unakuja.”

4 Naye Elifazi[f] Mtemani aka-
jibu, akasema:
2 “Mtu akijaribu kusema
nawe, je, utachoka?
Lakini ni nani anayeweza
kuzuia maneno?
3 Tazama! Umewarekebisha
wengi,[g]
Nawe ulikuwa ukiitia
nguvu[h] mikono iliyo
dhaifu.
4 Maneno yako yalimwinua
mtu yeyote mwenye
kujikwaa;[i]
Nawe uliyaimarisha magoti
yanayoyumba-yumba.[j]

SURA 3
a Zb 22:9
Lu 23:29
b Mhu 9:5
Mhu 9:10
c Ayu 30:23
Yoh 11:11
d 1Fa 2:10
2Nya 16:14
e Mwa 50:26
Isa 22:16
Eze 26:20
f Zb 58:8
Mhu 6:3
Ho 9:14
g Zb 49:19
h Zb 9:17
i Zb 146:4
Mhu 9:10
Isa 57:2
j Kut 5:6
k Ayu 30:23
Zb 49:10
Mhu 3:20
Mhu 8:8
Mhu 9:2
l 1Sa 1:10
2Fa 4:27
Met 31:6
m Hes 11:15
1Fa 19:4
Ayu 7:15
Yon 4:3
Ufu 9:6

Safu ya 2
a Ayu 19:8
b Ayu 12:14
Ayu 19:8
Omb 3:9
Ho 2:6
c Zb 80:5
Zb 102:9
d Zb 22:1
Zb 38:8
Isa 59:11
e Ayu 31:23

SURA 4
f Ayu 2:11
Ayu 42:9
g Lu 17:3
h Lu 22:32
i Met 12:18
Met 16:23
1Th 5:14
j Isa 35:3
Ebr 12:12

5 Lakini wakati huu
yanakupata wewe, nawe
unachoka;
Yanakugusa wewe, nawe
unaingiwa na wasiwasi.
6 Je, heshima yako kwa
Mungu siyo msingi wa
uhakika wako?
Je, tumaini lako silo
utimilifu[a] wa njia zako?
7 Tafadhali, kumbuka hili:
Je, ni nani aliyepata
kuangamia bila hatia?
Na wanyoofu[b] walipata
kufutiliwa mbali wapi?
8 Kulingana na yale
ambayo nimeona, wale
wanaotunga madhara
Na wale wanaopanda taabu
wataivuna wenyewe.[c]
9 Wao huangamia kupitia
pumzi ya Mungu,
Nao hufikia mwisho
kupitia roho ya hasira
yake.
10 Kuna mngurumo wa
simba, na sauti ya
mwana-simba,
Lakini meno ya
wana-simba wenye
manyoya shingoni
huvunjika.
11 Simba anaangamia kwa
kukosa mawindo,
Na watoto wa simba
hutenganishwa.
12 Sasa mimi nililetewa neno
kwa siri,
Na sikio langu likasikia
mnong'ono wake,[d]
13 Katika fikira
zinazofadhaisha
kutokana na maono ya
usiku,
Wakati usingizi mzito
unapowashika
wanadamu.

SURA 4

a Ayu 1:1

b Ayu 2:3
Ayu 42:7

c Ga 6:7

d 1Yo 4:1
Ufu 16:14

Safu ya 2

a Mwa 3:19

14 Hofu ilinishika, na
kutetemeka,
Nayo ikaijaza hofu mifupa
yangu iliyo mingi.
15 Na roho fulani ikapita juu
ya uso wangu;
Nywele za mwili wangu
zikaanza kusimama.
16 Ikaanza kusimama tuli,
Lakini sikuitambua sura
yake;
Umbo fulani lilikuwa mbele
ya macho yangu;
Kulikuwa na utulivu, na
sasa nikasikia sauti:
17 'Mwanadamu anayeweza
kufa—je, anaweza kuwa
mwenye haki kuliko
Mungu mwenyewe?
Au, je, mwanamume
anaweza kuwa safi kuliko
Mtengenezaji wake
mwenyewe?'
18 Tazama! Yeye hana imani
katika watumishi wake,
Naye huwashtaki wajumbe
wake kuwa na makosa.
19 Sembuse wale wanaokaa
katika nyumba za
udongo,
Ambao msingi wao umo
mavumbini![a]
Mtu huwaponda upesi
kuliko nondo.
20 Kuanzia asubuhi mpaka
jioni wao hupondwa
vipande-vipande;
Wao huangamia milele bila
yeyote kutia hilo moyoni.
21 Je, kamba yao ya hema
iliyo ndani yao
haikung'olewa?
Wao hufa kwa kukosa
hekima.

5 "Ita, tafadhali! Je, kuna
yeyote anayekujibu?
Nawe utamwendea nani
kati ya watakatifu?

2 Kwa maana usumbufu utamuua mpumbavu,
Na mtu anayeshawishiwa kwa urahisi wivu utamuua.
3 Mimi mwenyewe nimemwona mpumbavu akitia mizizi,[a]
Lakini ghafula nikaanza kuyalaani makao yake.
4 Wanawe wanakaa mbali na wokovu,[b]
Nao hupondwa langoni bila kuwa na mkombozi.
5 Kile anachovuna mwenye njaa hukila;
Na hata mtu hukichukua kutoka kwenye kulabu za mchinjaji,
Na kwa kweli mtego hukamata riziki yao.
6 Kwa maana madhara hayatoki katika mavumbi matupu,
Wala taabu haichipuki katika udongo mtupu.
7 Kwa maana mwanadamu huzaliwa kwa ajili ya taabu,
Kama vile cheche za moto zinavyoruka juu.
8 Hata hivyo, mimi mwenyewe ningetoa maombi kwa Mungu,
Nami ningempelekea Mungu takwa langu,[c]
9 Kwake Yeye anayetenda mambo makuu yasiyochunguzika,
Mambo ya ajabu yasiyo na hesabu;[d]
10 Kwake Yeye anayenyesha mvua juu ya uso wa dunia[e]
Na kupeleka maji juu ya mashamba;[f]
11 Kwake Yeye anayewaweka mahali pa juu wale walio chini,[g]
Hivi kwamba wale walio na huzuni wanakuwa juu katika wokovu;
12 Kwake Yeye anayevunja hila za werevu,
Hivi kwamba mikono yao haifanyi kazi ikawa na matokeo;[a]
13 Kwake Yeye anayewakamata wenye hekima katika ujanja wao wenyewe,[b]
Hivi kwamba shauri la watu werevu linafanywa haraka-haraka;[c]
14 Wanakutana na giza hata wakati wa mchana,
Nao wanapapasa-papasa katikati ya mchana kana kwamba ni usiku;[d]
15 Na kwake Yeye anayeokoa kutoka kwa upanga unaotoka kinywani mwao,
Na maskini kutoka kwa mkono wa mwenye nguvu,[e]
16 Hivi kwamba panakuwa na tumaini kwa ajili ya mtu wa hali ya chini,[f]
Lakini ukosefu wa uadilifu kwa kweli hufunga kinywa chake.[g]
17 Tazama! Ni mwenye furaha mtu yule ambaye Mungu humkaripia;[h]
Nawe usiikatae nidhamu ya Mweza-Yote!
18 Kwa maana yeye husababisha maumivu, lakini hulifunga jeraha;
Yeye huvunja vipande-vipande, lakini mikono yake huponya.
19 Yeye atakukomboa kutoka katika taabu sita,[i]
Na katika saba kitu chochote chenye kudhuru hakitakugusa.[j]

SURA 5
a Zb 37:35
b Zb 109:13 Zb 119:155
c Lu 18:11
d Zb 40:5 Zb 72:18 Ro 11:33
e Zb 65:9
f Ayu 26:8 Zb 147:8 Mdo 14:17
g Lu 1:52

Safu ya 2
a Ne 4:15
b 1Ko 3:19
c Zb 9:15
d Ayu 12:25 Met 4:19
e Zb 35:10
f 1Sa 2:8
g Zb 107:42
h Zb 94:12
i Zb 34:19
j Met 24:16

20 Yeye atakukomboa kutoka
katika kifo wakati wa
njaa,[a]
Na kutoka katika nguvu za
upanga wakati wa vita.
21 Utafichwa kutoka kwenye
pigo la ulimi,[b]
Nawe hutaogopa uporaji
unapokuja.
22 Utacheka uporaji na njaa,
Wala hutahitaji kuogopa
mnyama-mwitu wa
dunia.
23 Kwa maana agano lako
litakuwa pamoja na
mawe ya shambani,
Na mnyama wa mwituni
atafanywa aishi kwa
amani pamoja na wewe.[c]
24 Nawe hakika utajua
kwamba amani ndiyo
hema lako,
Nawe bila shaka utaenda
kuyaona malisho yako,
wala hutakosa chochote.
25 Nawe hakika utajua kuwa
uzao wako ni mwingi[d]
Na wazao wako kama
majani ya dunia.[e]
26 Utaingia kaburini ukiwa na
nguvu,[f]
Kama wakati miganda
inaporundikana wakati
wake.
27 Tazama! Hayo ndiyo
tumeyachunguza. Na
ndivyo yalivyo.
Uyasikie, nawe—uyajue
kwa ajili yako
mwenyewe."

6 Naye Ayubu akajibu,
akasema:
2 "Laiti usumbufu[g] wangu
ungepimwa,
Na wakati huohuo
wangeweka shida yangu
katika mizani!

SURA 5
a Mwa 45:7
b Met 12:18
Yak 3:8
c Law 26:6
d Zb 112:2
e Zb 72:16
f Kum 34:7

SURA 6
g Zb 31:9

Safu ya 2
a Yak 3:2
b Zb 38:2
c Met 18:14
d Zb 88:16
e Ayu 24:5
Yer 14:6
f Hes 11:15
1Fa 19:4
Ayu 3:21
Yon 4:3
g Ayu 3:22
h Zb 40:9
Mdo 20:27
i Law 19:2
Ho 11:9
1Pe 1:15
j Ayu 7:7
Zb 103:15

3 Kwa maana sasa ni nzito
hata kuliko mchanga wa
bahari.
Ndiyo sababu maneno
yangu mwenyewe
yamekuwa mazungumzo
ya ovyoovyo.[a]
4 Kwa maana mishale ya
Mweza-Yote iko nami,[b]
Ambayo roho yangu
inainywa sumu yake;[c]
Vitisho kutoka kwa Mungu
vinajipanga juu yangu.[d]
5 Je, punda-milia[e] atapaaza
kilio juu ya majani,
Au, je, ng'ombe atalia juu
ya chakula chake?
6 Je, vitu visivyo na ladha
vitaliwa bila chumvi,
Au, je, umajimaji wenye
utelezi wa mholi una
ladha yoyote?
7 Nafsi yangu imekataa
kugusa kitu chochote.
Ni kama ugonjwa ndani ya
chakula changu.
8 Laiti ombi langu lingekuja
Na kwamba Mungu
angenipa tumaini langu!
9 Na kwamba Mungu
angeniponda,
Kwamba angeuachilia
mkono wake na
kunikatilia mbali![f]
10 Bado ingekuwa ni faraja
yangu;
Nami ningeruka kwa
shangwe[g] kutokana na
maumivu yangu,
Hata ingawa hangekuwa
na huruma, kwa maana
sikuficha maneno[h] ya
Mtakatifu.[i]
11 Nguvu zangu ni nini, ndipo
niendelee kungojea?[j]
Na mwisho wangu ni
nini, ndipo niendelee
kurefusha nafsi yangu?

12 Je, nguvu zangu ni nguvu
za mawe?
Au, je, mwili wangu ni wa
shaba?
13 Je, ni kwamba mimi sina
uwezo wa kujipa msaada,
Na kazi yenye matokeo
imeondolewa mbali
nami?
14 Kwa habari ya mtu yeyote
anayezuia fadhili zenye
upendo kutoka kwa
mwenzake,[a]
Yeye pia ataachilia mbali
kumwogopa
Mweza-Yote.[b]
15 Ndugu zangu wametenda
kwa hila,[c] kama mto wa
majira ya baridi kali,
Kama mfereji wa mito
ya majira ya baridi kali
inayoendelea kukauka.
16 Ni myeusi kwa sababu ya
barafu,
Theluji hujificha juu yake.
17 Katika majira yake
hiyo hukosa maji,[d]
imenyamazishwa;
Kunapokuwa na joto kali
hiyo hukaushwa kutoka
mahali pake.[e]
18 Mapito ya njia yake
yanageuzwa kando;
Huenda juu katika mahali
patupu na kuangamia.
19 Misafara ya Tema[f]
imetazama,
Kundi la wasafiri la
Wasabea[g] limewangojea
wao.
20 Hakika wameona aibu
kwa sababu walikuwa
wametumaini;
Wamekuja mpaka mahali
hapo nao wanakata
tamaa.[h]
21 Kwa maana sasa ninyi
mmekuwa si kitu;[i]

SURA 6
a Met 3:3
Met 19:22
Ho 6:6
Zek 7:9
Mt 25:44
b Ayu 23:16
1Yo 3:17
c Ayu 19:19
Zb 38:11
d Yud 12
e Ayu 24:19
f Isa 21:14
Yer 25:23
g Ayu 1:15
h Yer 14:3
i Ayu 13:4

Safu ya 2
a Zb 38:11
b Mwa 14:16
c 2Sa 4:9
Zb 55:18
d Ayu 32:11
e Zb 19:12
Zb 19:13
Met 19:25
f Met 12:18
Met 25:11
g Ayu 16:3
Ayu 21:34
h Ayu 10:1
i Ayu 8:2
j Ayu 31:21
Mal 3:5
k Mwa 37:28
l Ayu 27:4
m Ayu 17:10

Mnaona hofu, nanyi
mnaogopa.[a]
22 Je, ni kwa sababu
nimesema, 'Nipe kitu,
Au, toeni zawadi kwa
ajili yangu kutoka katika
uwezo wenu;
23 Na mniokoe kutoka
mkononi mwa adui,[b]
Na mnikomboe kutoka
mkononi mwa
waonevu'?[c]
24 Mnifundishe, nami,
kwa upande wangu,
nitanyamaza;[d]
Na mnieleweshe kosa
ambalo nimetenda.[e]
25 Maneno ya unyoofu
yamekuwa—Si
machungu![f]
Lakini kukaripia kwenu
kunakaripia nini?[g]
26 Je, ninyi mnapanga hila ya
kukaripia maneno,
Wakati maneno ya mtu
aliyekata tamaa[h] ni kwa
ajili ya upepo tu?[i]
27 Ni kwa kadiri gani
mtaendelea kupiga kura
juu ya mtu asiye na
baba,[j]
Na kumtumia mwenzenu
kufanya biashara![k]
28 Na sasa mnisikilize mimi
kwa makini,
Na mwone ikiwa nitasema
uwongo[l] usoni penu.
29 Mrudi, tafadhali—ukosefu
wowote wa uadilifu
usitokee—
Ndiyo, rudini—uadilifu
wangu bado umo ndani
yake.[m]
30 Je, kuna ukosefu wa
uadilifu katika ulimi
wangu,
Au, je, kaakaa langu
halitambui shida?

7 "Je, duniani hakuna
kazi ya lazima[a] kwa
mwanadamu anayeweza
kufa,
Na je, siku zake si kama
siku za mfanyakazi wa
kukodiwa?[b]
2 Kama mtumwa, yeye
hupumua kwa kutamani
kivuli,[c]
Naye hungojea mshahara
wake kama mfanyakazi
wa kukodiwa.[d]
3 Ndivyo nilivyopewa miezi
ya ubatili,[e]
Nao wamenihesabia usiku
wenye taabu.[f]
4 Wakati ninapolala chini
nimesema, 'Nitaamka
wakati gani?'[g]
Na jioni inapoisha, pia
nimejawa na ukosefu
wa utulivu mpaka
mapambazuko ya
asubuhi.
5 Nyama yangu imefunikwa
na funza[h] na madonge ya
mavumbi;[i]
Ngozi yangu imefanyiza
vikoko na kuyeyuka.[j]
6 Siku zangu zimepita upesi[k]
kuliko chombo cha
mfumaji,
Nazo hufikia mwisho
katika hali ya ukosefu wa
tumaini.[l]
7 Kumbuka kwamba uzima
wangu ni upepo;[m]
Kwamba jicho langu
halitaona mema tena.
8 Jicho lake yeye anayeniona
halitanitazama;
Macho yako yatakuwa juu
yangu, lakini sitakuwapo.[n]
9 Wingu kwa hakika hufikia
mwisho wake na kwenda
zake;

SURA 7
a Ayu 14:14
b Ayu 14:6
Zb 39:4
c Isa 25:5
d Law 19:13
Kum 24:15
e Ayu 29:2
f Zb 6:6
g Ayu 2:8
Ayu 30:17
h Isa 14:11
i Ayu 30:19
j Ayu 30:30
k Zb 102:11
Zb 103:15
Zb 144:4
Yak 4:14
l Ayu 17:15
Ro 8:20
m Zb 89:47
Mhu 2:11
n Ayu 7:21
Yak 4:14

Safu ya 2
a Ayu 10:21
Ayu 14:12
Zb 78:39
Mhu 9:10
b Zb 103:16
Zb 146:4
Mhu 9:5
c 1Sa 1:10
Ayu 10:1
Met 14:10
d Ayu 38:8
e Ayu 3:21
Ufu 9:6
f Mwa 27:46
1Fa 19:4
Ayu 10:1
Yon 4:3
g Zb 62:9
Zb 144:4
Mhu 6:11
h Zb 8:4
Zb 103:15
Zb 144:3
Ebr 2:6

Ndivyo ambavyo yeye
anayeshuka katika
Kaburi* hatapanda juu.[a]
10 Hatarudi tena nyumbani
kwake,
Na mahali pake
hapatamtambua tena.[b]
11 Mimi pia sitazuia kinywa
changu.
Nitasema katika taabu ya
roho yangu;
Nitahangaikia uchungu wa
nafsi yangu![c]
12 Je, mimi ni bahari
au mnyama mkubwa wa
baharini,
Kwamba uweke mlinzi[d] juu
yangu?
13 Niliposema, 'Kitanda
changu kitanifariji,
Kitanda changu
kitanisaidia kuchukua
hangaiko langu,'
14 Hata hivyo umeniogopesha
kwa ndoto,
Nawe kupitia maono
hunifanya nishtuke kwa
woga,
15 Hivi kwamba nafsi yangu
inachagua kusongwa
pumzi,
Kifo[e] badala ya mifupa
yangu.
16 Nimekataa huo;[f] sitaishi
mpaka wakati usio na
kipimo.
Niache mimi, kwa sababu
siku zangu ni upepo wa
pumzi.[g]
17 Mwanadamu anayeweza
kufa[h] ni kitu gani ili
kwamba umlee,
Na ndipo uuweke moyo
wako juu yake,
18 Na ndipo umkazie
uangalifu kila asubuhi,

Ayu 7:9* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

Ndipo umjaribu kila
dakika?[a]
19 Kwa nini huachi kunikazia
macho,[b]
Wala hata uniache mpaka
nimeze mate yangu?
20 Ikiwa nimetenda dhambi,
ni nini ninaloweza
kutimiza kukupinga
wewe, Ee Mtazamaji wa
wanadamu?[c]
Kwa nini umeniweka
kuwa shabaha yako, hivi
kwamba niwe mzigo
kwako?
21 Na kwa nini usisamehe
ukosaji wangu[d]
Na kuliachilia kosa langu?
Kwa maana sasa nitalala
chini mavumbini;[e]
Nawe hakika utanitafuta,
nami sitakuwapo."

8 Naye Bildadi Mshua[f] akaji-
bu, akasema:
2 "Utaendelea kusema
mambo haya mpaka
wakati gani,[g]
Wakati maneno ya kinywa
chako ni upepo mtupu
wenye nguvu?[h]
3 Je, Mungu mwenyewe
atapotosha hukumu,[i]
Au, je, Mweza-Yote
atapotosha uadilifu?[j]
4 Ikiwa wana wako
mwenyewe
wamemtendea dhambi,
Hivi kwamba anawaacha
waingie mkononi mwa
maasi yao,
5 Ikiwa wewe mwenyewe
utamtafuta Mungu,[k]
Na ikiwa utamwomba kwa
bidii kibali Mweza-Yote,
6 Ikiwa wewe ni safi na
mnyoofu,[l]
Kufikia sasa angeamka
kwa ajili yako

SURA 7

a Kum 13:3
Ayu 23:10
Zb 7:9

b Ayu 14:6

c Ayu 34:21
Met 5:21
Yer 16:17
Ebr 4:13
1Pe 3:12

d Isa 33:24

e Mwa 3:19
Zb 104:29
Mhu 12:7
Da 12:2

SURA 8

f Mwa 25:2
1Nya 1:32
Ayu 42:9

g Ayu 11:3

h Ayu 6:26

i Mwa 18:25
Ayu 34:12

j Kum 32:4
2Nya 19:7

k Ayu 5:8
Ayu 11:13
Ayu 22:23

l Ayu 1:8
Ayu 6:24

Safu ya 2

a Ayu 42:12

b Ayu 11:17
Zb 39:5

c Ayu 15:18

d Mwa 47:9

e 1Nya 29:15
Ayu 14:1
Zb 144:4

f Kut 2:3
Isa 18:2
Isa 35:7

g Zb 129:6

h Ayu 42:7
Zb 9:17

i Ayu 27:8

j Isa 59:5

Naye hakika angerudisha
makao yako ya uadilifu.
7 Pia, huenda ikawa mwanzo
wako ulikuwa jambo
dogo,
Lakini mwisho wako
baadaye ungekuwa
mkubwa sana.[a]
8 Kwa kweli, tafadhali uliza
wale wa kizazi cha
zamani,[b]
Nawe uelekeze fikira
zako kwenye mambo
ambayo baba zao
waliyachunguza.[c]
9 Kwa maana sisi ni wa jana
tu,[d] wala hatujui lolote,
Kwa sababu siku zetu
duniani ni kivuli.[e]
10 Je, wao wenyewe
hawatakufundisha,
wakuambie,
Na je, hawatatoa maneno
kutoka moyoni mwao?
11 Je, mmea wa mafunjo[f]
utakua uwe mrefu
mahali pasipo na
majimaji?
Je, tete litakua liwe kubwa
bila maji?
12 Wakati lingali tumba,
ambalo halijakatwa,
Litakauka kabla ya majani
mengine yote.[g]
13 Ndivyo zilivyo njia za
wale wote wanaomsahau
Mungu,[h]
Na tumaini la mwasi-imani
litaangamia,[i]
14 Ambaye uhakika wake
hukatiliwa mbali,
Na ambaye tegemeo lake ni
nyumba ya buibui.[j]
15 Ataegemea juu ya nyumba
yake, lakini haitaendelea
kusimama;
Ataishika, lakini
haitadumu.

16 Amejaa utomvu mbele ya jua,
Na tawi lake huchipuka shambani mwake.[a]
17 Mizizi yake husokotana ndani ya rundo la mawe,
Anatazama nyumba ya mawe.
18 Mtu akimmeza kutoka mahali pake,[b]
Hiyo pia hakika itamkana, ikisema, 'Sijakuona wewe.'[c]
19 Tazama! Huko ndiko kuyeyuka kwa njia yake;[d]
Na wengine huchipuka kutoka mavumbini.
20 Tazama! Mungu mwenyewe hatamkataa mtu yeyote asiye na lawama,
Wala hataushika mkono wa watenda-maovu,
21 Mpaka atakapojaza kinywa chako kicheko,
Na midomo yako sauti ya shangwe.
22 Wale hasa wanaokuchukia watavikwa aibu,[e]
Na hema la waovu halitakuwapo."

9 Naye Ayubu akajibu, akasema:
2 "Kwa kweli najua ya kuwa iko hivyo.
Lakini mwanadamu anayeweza kufa anawezaje kuwa upande wa haki akiwa katika kesi na Mungu?[f]
3 Akipendezwa kushindana naye,[g]
Hawezi kumjibu mara moja kati ya elfu moja.
4 Yeye ni mwenye hekima moyoni na mwenye nguvu katika uwezo.[h]
Ni nani anayeweza kumwonyesha ukaidi naye atoke bila madhara?[a]
5 Yeye anaiondoa milima,[b]
hivi kwamba watu hata wasijue kuihusu,
Yeye ambaye ameipindua katika hasira yake.[c]
6 Yeye anaiondoa dunia ikiwa inatetemeka kutoka mahali pake,
Hivi kwamba nguzo[d] zake zinatetemeka.
7 Yeye analiambia jua lisiangaze,
Naye anatia muhuri kuzizunguka nyota,[e]
8 Anatandaza mbingu akiwa peke yake[f]
Na kuyakanyaga mawimbi makubwa ya bahari;[g]
9 Anafanyiza kundi-nyota la Ashi, kundi-nyota la Kesili,
Na kundi-nyota la Kima[h] na vyumba vya ndani vya Kusini;
10 Anafanya mambo makuu yasiyochunguzika,[i]
Na mambo ya ajabu yasiyo na hesabu.[j]
11 Tazama! Yeye anapita kando yangu nami simwoni,
Naye anasonga mbele nami simtambui.[k]
12 Tazama! Ananyakua.
Ni nani anayeweza kumpinga?
Ni nani atakayemwambia, 'Unafanya nini?'[l]
13 Mungu mwenyewe hatageuza hasira yake;[m]
Wasaidizi wa mshambuliaji[n] watainama chini yake.

SURA 8
a Ayu 5:3; Zb 37:35
b Ayu 7:10
c Ayu 20:9
d Ayu 20:5
e Zb 35:26

SURA 9
f Kum 32:4; Zb 143:2; Ro 3:23
g Ayu 40:2; Ro 9:20
h Ayu 36:5; Zb 104:24; Isa 40:26; Da 2:20

Safu ya 2
a Met 14:16; Met 28:14; Isa 30:1; Da 5:20; Zek 7:12; Ro 2:5; 1Ko 10:22
b Ayu 28:9
c Yer 10:10; Hab 3:6
d Zb 75:3
e Mwa 1:16; Eze 32:7
f Mwa 1:1; Zb 33:6; Isa 44:24
g Ayu 38:11
h Ayu 38:31; Amo 5:8
i Ayu 5:9; Isa 40:28; Ro 11:33
j Zb 40:5
k Ayu 23:8; Yoh 1:18
l Da 4:35; Ro 9:20
m Kum 32:22; Yer 17:4
n Ayu 26:12; Isa 51:9

14 Ni zaidi sana hivyo mimi
mwenyewe nikimjibu!
Nitachagua maneno yangu
nitakayosema naye,[a]
15 Ambaye siwezi kumjibu,
hata ingawa ningekuwa
upande wa haki.[b]
Ningeomba kibali kwa bidii
kutoka kwa mpinzani
wangu katika kesi.[c]
16 Kama ningemwita, je,
angenijibu?[d]
Siamini kwamba angetega
sikio kuisikiliza sauti
yangu;
17 Ambaye ananichubua kwa
dhoruba
Na kwa hakika kuzidisha
majeraha yangu bila
sababu.[e]
18 Hataniruhusu nipumue
pumzi safi,[f]
Kwa kuwa anaendelea
kunijaza sana mambo
machungu.
19 Ikiwa mtu yeyote ni
mwenye nguvu katika
uwezo, pale yeye yupo;[g]
Na ikiwa yeyote ni mwenye
nguvu katika haki, laiti
ningeitwa!
20 Kama ningekuwa upande
wa haki, kinywa changu
mwenyewe
kingenitangaza kuwa
mwovu;
Kama ningekuwa bila
lawama, basi yeye
angenitangaza kuwa
mpotovu.
21 Kama ningekuwa bila
lawama, nisingeijua nafsi
yangu;
Ningeukataa uhai wangu.
22 Kuna jambo moja. Ndiyo
sababu ninasema,
'Anamkomesha mtu asiye
na lawama, pia mtu
mwovu.'[h]

SURA 9

a Zb 19:14
b Ayu 10:15
c Mt 5:25
Lu 12:58
d Zb 102:17
Met 15:29
e Ayu 2:3
Ayu 34:6
f Ayu 27:3
g Isa 40:28
h Mhu 9:2

Safu ya 2

a 1Yo 5:19
b Ayu 7:6
Zb 90:10
Yak 4:14
c Hab 1:8
d Ayu 7:13
e Met 15:13
f Ayu 21:6
g Zb 73:13
Yer 2:35
h Yer 2:22
Mal 3:2
i Hes 23:19
Isa 45:9
Yer 49:19
Ro 9:20

23 Furiko la ghafula
likisababisha kifo kwa
ghafula,
Yeye angefanyia mzaha
kukata tamaa kwa watu
wasio na hatia.
24 Dunia imetiwa mkononi
mwa mwovu;[a]
Anaufunika uso wa
waamuzi wake.
Kama si yeye, basi, ni nani?
25 Pia siku zangu zimeenda
upesi kuliko mkimbiaji;[b]
Zimekimbia, hakika
hazitaona mema.
26 Zimesonga mbele kama
mashua za matete,
Kama tai ambaye huruka
huku na huku kwa ajili
ya chakula.[c]
27 Ikiwa nimesema, 'Acha
nisahau hangaiko langu,[d]
Acha nibadili sura[e] yangu
na kuchangamka,'
28 Nimeogopa maumivu
yangu yote;[f]
Ninajua kwamba
hutanihesabu kuwa sina
hatia.
29 Mimi mwenyewe nitakuwa
mwovu.
Kwa nini ninataabika kwa
ubatili mtupu?[g]
30 Ikiwa kwa kweli
ningejiosha katika maji
ya theluji,
Nami kwa kweli nisafishe
mikono yangu katika
sabuni,[h]
31 Ndipo wewe ungenichovya
katika shimo,
Na mavazi yangu kwa
hakika yangenichukia.
32 Kwa kuwa yeye si
mwanadamu[i] kama mimi
ndipo nimjibu,
Kwamba tuje pamoja
katika hukumu.

33 Hakuna mtu yeyote wa
kutuamua,[a]
Kwamba atie mkono wake
juu yetu sisi wawili.
34 Acha aiondoe fimbo yake
kutoka juu yangu,[b]
Na kuogopesha kwake,
kusinitie hofu.
35 Acha niseme wala
nisimwogope,
Kwa maana mimi
mwenyewe sina
mwelekeo huo.

10 "Nafsi yangu inahisi
kuchukizwa na uhai
wangu.[c]
Nitaonyesha hangaiko
langu kujihusu
mwenyewe.
Nitasema kwa uchungu
wa nafsi yangu!
2 Nitamwambia Mungu,
'Usinitangaze kuwa
mwovu.
Nijulishe kwa nini
unashindana nami.
3 Je, ni vema kwako kwamba
wewe utende kosa,[d]
Kwamba ukatae tokeo la
kazi yenye nguvu ya
mikono yako,[e]
Na kwamba kwa kweli
uangazie shauri la
waovu?
4 Je, una macho[f] ya nyama,
Au, je, wewe unaona kama
anavyoona mwanadamu
anayeweza kufa?[g]
5 Je, siku zako ni kama
siku za mwanadamu
anayeweza kufa,[h]
Au, miaka yako ni kama
siku za mwanamume,
6 Kwamba ujaribu kutafuta
kosa langu
Nawe uendelee kuitafuta
dhambi yangu?[i]

SURA 9
a 1Sa 2:25
1Ti 2:5
b Ayu 13:21
Zb 39:10

SURA 10
c Hes 11:15
1Fa 19:4
Ayu 7:16
Yon 4:3
Ro 8:20
d Mwa 18:25
Kum 32:4
Ro 3:8
e Ayu 14:15
Zb 138:8
Isa 64:8
f Zb 11:4
g 1Sa 16:7
h Zb 90:2
Yer 10:10
Ebr 1:12
i Ayu 10:14
Ro 3:12

Safu ya 2
a Ayu 1:8
Zb 139:1
b Kum 32:39
c Zb 119:73
Zb 139:13
Zb 139:15
d Mwa 2:7
Isa 45:9
Ro 9:21
e Mwa 3:19
Zb 104:29
Mhu 12:7
f Isa 64:8
g Zb 139:15
h Zb 139:16
i Zb 8:4
j Zb 139:1
k Hes 14:18
l Isa 3:11
m Ayu 9:15
Lu 17:10
n Zb 25:18
Zb 119:153
o 2Sa 22:28
Ayu 40:11
Isa 2:11
Lu 1:51
Yak 4:6
p Isa 38:13

7 Ijapokuwa unajua kwamba
mimi sina kosa,[a]
Na hakuna yeyote
anayekomboa kutoka
mkononi mwako?[b]
8 Mikono yako mwenyewe
imeniunda hivi kwamba
ikanifanyiza mimi[c]
Mzima pande zote, na bado
unataka kunimeza.
9 Tafadhali, kumbuka
kwamba umenifanyiza
kutoka katika udongo[d]
Nawe utanifanya nirudi
katika mavumbi.[e]
10 Je, hukunimwaga kama
maziwa
Na kunigandisha kama
jibini?[f]
11 Ulinivika ngozi na nyama
Ukanifuma kwa mifupa na
kano.[g]
12 Umenipa uzima na fadhili
zenye upendo;[h]
Na uangalizi[i] wako
mwenyewe umeilinda
roho yangu.
13 Nawe umeficha mambo
hayo moyoni mwako.
Ninajua vema kwamba una
mambo hayo.
14 Ikiwa nimetenda dhambi
na umeendelea
kunitazama[j]
Nawe hunichukulii kuwa
sina hatia katika kosa
langu;[k]
15 Ikiwa kweli nimekosea, ole
wangu![l]
Na ikiwa kweli niko
upande wa haki, nisipate
kuinua kichwa changu,[m]
Nikiwa nimejawa sana na
aibu na kujawa na
mateso.[n]
16 Nacho kikitenda kwa
majivuno,[o] utaniwinda
kama mwana-simba,[p]

Nawe utajionyesha tena
kuwa wa ajabu kwangu.
17 Utaleta mashahidi wako
wapya mbele yangu,
Nawe utafanya usumbufu
wako kuwa mkubwa
zaidi juu yangu;
Magumu baada ya magumu
yako pamoja nami.
18 Basi kwa nini ulinitoa nje
ya tumbo la uzazi?[a]
Kama ningekata pumzi, ili
hata jicho lisinione,
19 Ningekuwa kana kwamba
sijapata kuwako;
Ningeletwa kutoka
tumboni mpaka
kaburini.'
20 Je, siku zangu si chache?[b]
Na aachilie mbali,
Na aache kunikazia macho,
ili ning'ae[c] kidogo
21 Kabla sijaenda
zangu—nami sitarudi[d]—
Kwenye nchi ya giza na
kivuli kizito,[e]
22 Kwenye nchi ya giza kama
weusi, ya kivuli kizito
Na ya mchafuko, ambako
hakuangazi zaidi ya
weusi."

11 Naye Sofari Mnaamathi[f]
akajibu, akasema:
2 "Je, maneno mengi
yatakosa kujibiwa,
Au, je, mwenye kujisifu
tu atakuwa upande wa
haki?
3 Je, maongezi yako matupu
yatawanyamazisha watu,
Na je, utaendelea kudharau
bila kuwa na mtu wa
kukukemea?[g]
4 Pia unasema, 'Mafundisho
yangu[h] ni safi,
Nami nimeonekana safi[i]
kwelikweli machoni
pako.'

SURA 10
a Ayu 3:11
Yer 20:18
b Ayu 7:6
Ayu 14:1
Zb 39:5
Zb 103:15
c Ayu 9:27
Zb 39:13
d Ayu 7:9
Zb 115:17
Isa 38:11
e Ayu 3:5
Ayu 38:17
Zb 23:4
Zb 88:12
Mhu 9:10

SURA 11
f Ayu 42:9
g Ayu 12:4
h Ayu 6:10
i Ayu 6:29
Ayu 10:7

Safu ya 2
a Ayu 38:1
b Ezr 9:13
c Mhu 3:11
Ro 11:33
d Zb 139:8
e Zb 94:11
Sef 3:5

5 Na bado, laiti Mungu
mwenyewe angesema
Na kukufungulia midomo
yake![a]
6 Ndipo angekuambia siri za
hekima,
Kwa kuwa mambo ya
hekima inayotumika ni
mengi.
Pia, ungejua kwamba
Mungu anaruhusu
sehemu ya makosa yako
yasahaulike kwa ajili
yako.[b]
7 Je, unaweza kuvumbua
mambo yenye kina ya
Mungu,[c]
Au, je, unaweza kuvumbua
kikomo chenyewe cha
Mweza-Yote?
8 Iko juu kuliko mbingu.
Wewe unaweza kutimiza
nini?
Ina kina kirefu kuliko
Kaburi.*[d] Wewe unaweza
kujua nini?
9 Ina kipimo kirefu kuliko
dunia,
Na ni pana kuliko bahari.
10 Akisonga mbele na
kumshika mtu
Na kuita mahakama,
basi ni nani anayeweza
kumpinga?
11 Kwa kuwa yeye mwenyewe
anajua vema watu
wasiosema kweli.[e]
Anapoona jambo lenye
kudhuru, je, yeye pia
hatalikazia uangalifu?
12 Hata mtu asiye na akili
atapata kusudi jema
Mara tu punda-mwitu
anapozaliwa kuwa
mwanadamu.

Ayu 11:8* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

13 Wewe mwenyewe
ukitayarisha moyo wako
kwelikweli
Na kwa kweli umnyooshee
mikono yako,[a]
14 Ikiwa jambo lenye kudhuru
limo mkononi mwako,
liondolee mbali kabisa,
Wala usiache ukosefu wa
uadilifu ukae katika
mahema yako.
15 Kwa maana ndipo
utakapoinua uso wako
bila kasoro[b]
Nawe hakika utafanywa
imara, wala hutaogopa.
16 Kwa maana
wewe—utaisahau taabu;
Utaikumbuka kama maji
ambayo yamepita.
17 Na urefu wa maisha yako[c]
utainuka kwa wangavu
kuliko katikati ya
mchana;
Giza litakuwa kama
asubuhi.[d]
18 Nawe utakuwa na tegemeo
kwa maana kuna
tumaini;
Nawe utatazama huku
na huku kwa
uangalifu—utalala kwa
usalama.[e]
19 Nawe hakika utalala
na kujinyoosha, pasipo
mtu yeyote wa
kukutetemesha.
Na hakika watu wengi
watakutuliza;[f]
20 Nayo macho ya waovu
yataisha nguvu;[g]
Na hakika mahali pa
kukimbilia pataangamia
kutoka kwao,[h]
Na tumaini lao litakuwa
ni kukata pumzi kwa
nafsi."[i]

SURA 11
a Zb 143:6
b Mwa 4:5
c Zb 39:5
Zb 89:47
d Zb 112:4
Isa 58:8
e Law 26:6
Zb 3:5
Met 3:24
f Zb 45:12
g Law 26:16
h Ayu 8:14
Ayu 18:14
i Ufu 9:6

Safu ya 2

SURA 12
a Isa 5:21
b Ayu 13:2
Met 2:10
c 2Ko 11:5
d Ayu 16:10
Ayu 17:2
Ayu 30:1
Zb 22:7
Ebr 11:36
e Zb 91:15
Mik 7:7
f Met 13:9
g Kum 32:35
h Ayu 21:7
Zb 37:35
Zb 73:12
Yer 12:1
i Amu 17:5
j Met 6:6
Isa 1:3
Ro 1:20
k Yer 8:7
l Zb 19:4
Zb 148:9
m Mwa 1:20

12 Naye Ayubu akajibu,
akasema:
2 "Kwa kweli ninyi ndinyi
watu,
Na hekima itakufa pamoja
nanyi![a]
3 Mimi pia nina moyo[b] kama
ninyi.
Mimi si mdogo kuliko
ninyi,[c]
Na ni nani asiye na mambo
kama hayo?
4 Ninakuwa mtu wa
kudhihakiwa na
wenzake,[d]
Mtu anayemwita Mungu ili
amjibu.[e]
Mtu mwadilifu, asiye na
lawama, amekuwa wa
kudhihakiwa.
5 Katika fikira zake, mtu
asiye na mahangaiko
hudharau maangamizi;[f]
Yametayarishwa kwa ajili
ya wale wenye miguu
inayoyumba-yumba.[g]
6 Mahema ya waporaji
hayana wasiwasi,[h]
Na wale wanaomtia Mungu
ghadhabu wana usalama
Ulio wa mtu ambaye
ameleta mungu mkononi
mwake.[i]
7 Hata hivyo, tafadhali uliza
wanyama wa kufugwa,
nao watakufundisha;[j]
Pia viumbe vya mbinguni
vyenye mabawa, navyo
vitakuambia.[k]
8 Au onyesha kupendezwa
kwako na dunia, nayo
itakufundisha;[l]
Na samaki wa baharini[m]
watakutangazia.
9 Ni nani kati ya hao wote
ambaye hajui vema

Kwamba ni mkono wa
Yehova ambao umefanya
haya,[a]
10 Ambaye mkononi mwake
mna nafsi[b] ya kila aliye
hai
Na roho ya mwili wote wa
mwanadamu?[c]
11 Je, sikio halipimi maneno[d]
Kama kaakaa[e] linavyoonja
chakula?
12 Je, hekima haimo katikati
ya wazee[f]
Na uelewaji katika wingi
wa siku?
13 Yeye ana hekima na
nguvu;[g]
Ana shauri na uelewaji.[h]
14 Tazama! Yeye hubomoa, ili
pasiwe na ujenzi;[i]
Yeye huifunga kwa ajili
ya mwanadamu, ili
isifunguliwe.[j]
15 Tazama! Yeye huweka
kizuizi juu ya maji nayo
hukauka;[k]
Naye huyapeleka, nayo
huibadili dunia.[l]
16 Yeye ana nguvu na hekima
inayotumika;[m]
Yeye anayefanya kosa na
yeye anayepotosha ni
wake;[n]
17 Anafanya washauri
watembee miguu wazi,[o]
Naye hufanya waamuzi
wawe na wazimu.
18 Yeye kwa kweli hufungua
vifungo vya wafalme,[p]
Naye hufunga viuno vyao
mshipi.
19 Yeye anawafanya
makuhani watembee
miguu wazi,[q]
Naye huwapindua wale
walioketi daima;[r]
20 Yeye anaondoa usemi
kutoka kwa waaminifu,
Naye huondolea mbali akili
ya watu wazee;
21 Yeye anamwaga dharau juu
ya watu wenye vyeo,[a]
Naye hulegeza mshipi wa
wenye nguvu;
22 Yeye anafunua mambo
mazito kutoka katika
giza,[b]
Naye huleta kivuli kizito
kwenye nuru;
23 Anafanya mataifa kuwa
makubwa, ili ayaharibu;[c]
Anaeneza mataifa, ili
ayaondoe;
24 Anaondoa moyo wa walio
vichwa vya watu wa nchi,
Ili aweze kuwafanya
watange-tange katika
mahali patupu,[d] pasipo
na njia.
25 Wao hupapasa gizani,[e]
pasipo na nuru,
Ili aweze kuwafanya
watange-tange kama
mlevi.[f]

13 "Tazama! Jicho langu
limeona hayo yote,
Sikio langu limesikia
nalo linayafikiria.
2 Mambo ambayo ninyi
mnajua hata mimi
nayajua vema pia;
Mimi si mdogo kuliko
ninyi.[g]
3 Hata hivyo mimi,
kwa upande wangu,
ningesema na
Mweza-Yote mwenyewe,[h]
Nami ningependezwa
kuhojiana na Mungu.
4 Kwa upande mwingine,
ninyi ni watu wa kupaka
uwongo;[i]
Ninyi nyote ni matabibu
wasio na faida.[j]

SURA 12
a Yer 27:5 Ro 11:36
b Eze 18:4
c Hes 16:22 Zb 104:30 Mhu 12:7 Da 5:23
d 1Ko 10:15
e Ayu 34:3
f Law 19:32 Ayu 32:7 Met 16:31 Met 20:29
g Ayu 9:4 Ayu 36:5 Isa 44:25 Da 2:20
h Zb 147:5 Isa 40:14 Yer 10:12 Ro 11:34
i Isa 31:2 Yer 51:64 Mal 1:4 Yud 7
j Isa 22:22
k Mwa 8:1 Kut 14:21 Nah 1:4
l Mwa 6:17 1Fa 8:36 Zb 104:8
m Ayu 12:13 Ro 1:20
n 1Fa 22:22
o Isa 29:14 Isa 44:25
p Da 2:21
q Yer 14:18 Yer 52:24
r Lu 1:52

Safu ya 2
a Zb 107:40
b Da 2:22 Mt 10:26 1Ko 4:5
c Ufu 16:14
d Zb 107:4 Zb 107:40
e Kum 28:29 1Yo 2:11
f Zb 107:27

SURA 13
g Ayu 12:3 2Ko 11:5
h Ayu 23:3 Ayu 29:4 Ayu 31:35
i Zb 119:69
j Ayu 6:21 Ayu 16:2 Yer 6:14 Eze 34:4

5 Laiti mngenyamaza kabisa,
Ili iwe hekima kwa upande wenu![a]
6 Tafadhali, sikieni hoja zangu za kujibu,[b]
Na msikilize kwa makini maombi ya midomo yangu.
7 Je, ninyi mtasema maneno ya ukosefu wa uadilifu kwa ajili ya Mungu mwenyewe,
Na je, mtasema udanganyifu kwa ajili yake?[c]
8 Je, mtamtendea kwa upendeleo,[d]
Au, je, kwa ajili ya Mungu wa kweli mtashindana katika kesi?
9 Je, ingekuwa vema kwamba awachunguze ninyi?[e]
Au, je, mtacheza na yeye kama mtu anavyocheza na mwanadamu anayeweza kufa?
10 Hakika atawakaripia ninyi[f]
Ikiwa mnajaribu kuonyesha ubaguzi kisiri;[g]
11 Je, utukufu wake hautawafanya mshtuke kwa woga,
Na hofu yake ianguke juu yenu?[h]
12 Maneno yenu ya kukumbukwa ni methali za majivu;
Vinundu vya ngao zenu ni kama vinundu vya ngao vya udongo.[i]
13 Nyamazeni mbele yangu, ili mimi mwenyewe nipate kusema.
Kisha na lije juu yangu jambo lolote lile!

SURA 13
a Met 17:28 Yak 1:19
b Met 18:13
c Yer 14:14
d Met 24:23
e Zb 139:23 Yer 17:10
f Zb 50:21
g Zb 82:2 Yak 2:9
h Ne 5:9
i Ayu 4:19

Safu ya 2
a Amu 12:3 1Sa 19:5 Zb 119:109
b Ayu 19:25 Zb 23:4
c Kut 15:2 Zb 27:1 Isa 12:2
d Ayu 8:13 Ayu 27:8 Ayu 36:13 Zb 24:3 Isa 33:14
e Met 18:13
f 1Ko 10:12
g Ayu 33:6 Isa 50:8
h Ayu 33:7
i Ayu 9:34 Zb 119:120 Ebr 10:31
j Zb 10:1 Zb 13:1 Zb 44:24
k Omb 2:5

14 Kwa nini ninabeba nyama ya mwili wangu katika meno yangu
Na kutia nafsi yangu mwenyewe mkononi mwangu?[a]
15 Hata kama angeniua, je, singengojea?[b]
Ningetoa hoja tu usoni pake kwa ajili ya njia zangu.
16 Yeye pia angekuwa wokovu wangu,[c]
Kwa maana hakuna mwasi-imani yeyote atakayekuja mbele zake.[d]
17 Sikieni neno langu kabisa,[e]
Na tangazo langu liwe masikioni mwenu.
18 Tazama! Tafadhali, nimeleta kesi ya haki;[f]
Ninajua vema kwamba mimi mwenyewe niko upande wa haki.
19 Ni nani atakayeshindana na mimi?[g]
Kwa maana sasa kama ningenyamaza kimya ningekata pumzi tu!
20 Ila tu usinitendee mambo mawili;
Hapo basi sitajificha kwa sababu yako tu;[h]
21 Ondoa mkono wako mbali sana kutoka juu yangu,
Na hofu kutoka kwako—isinitie woga.[i]
22 Ama uite ili mimi mwenyewe nijibu;
Au mimi niseme, nawe unipe jibu.
23 Mimi nina makosa na dhambi kwa njia gani?
Nijulishe maasi yangu na dhambi yangu.
24 Kwa nini unaficha uso wako[j]
Na kuniona mimi kama adui yako?[k]

25 Je, utafanya jani
linalopeperushwa
litetemeke,
Au kuendelea kuyafukuza
majani makavu tu?
26 Kwa maana unaendelea
kuandika juu yangu
mambo machungu[a]
Nawe unanifanya niyapate
matokeo ya makosa ya
ujana wangu.[b]
27 Pia unaendelea kuiweka
miguu yangu katika
mikatale,[c]
Nawe unaziangalia njia
zangu zote;
Unatia alama ya mstari
wako kwa ajili ya nyayo
za miguu yangu.
28 Naye ni kama
kitu kilichooza ambacho
huchakaa;[d]
Kama vazi ambalo nondo
kweli hula.[e]

14 "Mwanadamu,
aliyezaliwa na
mwanamke,[f]
Ana maisha mafupi[g]
na yenye kujaa
msukosuko.[h]
2 Amechanuka kama ua na
kukatiliwa mbali,[i]
Naye hukimbia kama
kivuli[j] wala haendelei
kuwako.
3 Ndiyo, umefungua macho
yako juu ya huyu,
Nami unanitia katika
hukumu[k] pamoja na
wewe.
4 Ni nani anayeweza
kutokeza mtu safi
kutoka katika mtu asiye
safi?[l]
Hakuna hata mmoja.
5 Ikiwa siku zake
zimeamuliwa,[m]

SURA 13
a Kum 32:32
Ru 1:20
Ayu 16:9
Ayu 19:11
Ayu 33:10
b Zb 25:7
Yer 31:19
c Ayu 33:11
d Ho 5:12
e Zb 39:11
Isa 50:9
Yak 5:2

SURA 14
f Zb 51:5
1Ko 11:12
g Zb 39:5
Zb 90:10
Yak 4:14
h Mwa 3:19
Mwa 47:9
Mhu 2:23
i Zb 103:15
Isa 40:6
Yak 1:10
1Pe 1:24
j 1Nya 29:15
Zb 102:11
Zb 144:4
Mhu 8:13
k Zb 143:2
l Mwa 5:3
Zb 51:5
Yoh 3:6
Ro 5:12
m Zb 39:4
Lu 12:20

Safu ya 2
a Zb 39:13
b Isa 11:1
Da 4:26
Da 11:7
c Zb 1:3
d 1Ko 15:36
e Mwa 49:33
Mhu 3:19
Mhu 9:10
f Ayu 6:17
Yer 15:18
g Mhu 9:5
Mhu 12:5
h Isa 51:6
Ebr 1:11
i Zb 13:3
Yer 51:39
Yoh 11:11
Mdo 7:60
j Mwa 44:29
1Sa 2:6
Isa 57:2
k Yoh 5:28
l Lu 23:42
Ebr 11:35

Hesabu ya miezi yake iko
kwako;
Umeweka amri kwa ajili
yake ili asiweze kuvuka.
6 Geuza macho yako kutoka
kwake ili apumzike,[a]
Mpaka apate raha kama
mfanyakazi wa kukodiwa
anavyopata katika siku
yake.
7 Kwa maana hata kwa ajili
ya mti kuna tumaini.
Ukikatwa, utachipuka
tena,[b]
Na tawi lake halitakoma.
8 Mzizi wake ukizeeka
katika udongo
Na kisiki chake kikifa
katika mavumbi,
9 Utachipuka unaponusa
harufu ya maji[c]
Nao utatokeza tawi kama
mmea mpya.[d]
10 Lakini mwanamume hufa
na kulala akiwa
ameshindwa;
Na mtu wa udongo hukata
pumzi, naye yuko wapi?[e]
11 Maji hupotea kutoka
baharini,
Na mto hutiririka na
kukauka.[f]
12 Mwanadamu pia hulala
chini wala haamki.[g]
Hawataamka mpaka
mbingu itakapokuwa
haipo tena,[h]
Wala hawataamshwa
katika usingizi wao.[i]
13 Laiti ungenificha katika
Kaburi,*[j]
Kwamba ungenificha
mpaka hasira yako
igeuke,
Kwamba ungeniwekea
kikomo cha wakati[k] na
kunikumbuka![l]

Ayu 14:13* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

14 Mtu akifa, je, anaweza
kuishi tena?[a]
Mimi nitangojea siku zote
za kazi yangu ya
kulazimishwa,[b]
Mpaka kitulizo changu
kije.[c]
15 Wewe utaita, na mimi
mwenyewe nitakujibu.[d]
Kwa kuwa utaitamani sana
kazi ya mikono yako.
16 Kwa maana sasa
unaendelea kuhesabu
hatua zangu;[e]
Hutazami lolote isipokuwa
dhambi yangu.[f]
17 Maasi yangu yamefungwa
kwa muhuri katika
mfuko,[g]
Nawe unatia gundi juu ya
kosa langu.
18 Hata hivyo, mlima,
unaoanguka, utafifia,
Na hata mwamba
utaondolewa mahali
pake.
19 Maji kwa hakika yanakula
hata mawe;
Kumwagika kwake
kunayachukua mavumbi
ya dunia.
Ndivyo ulivyoliharibu
tumaini la mwanadamu
anayeweza kufa.
20 Unamshinda milele hivi
kwamba yeye anaenda
zake;[h]
Unauharibu uso wake
hivi kwamba unamwacha
aende zake.
21 Wanawe hupewa heshima,
lakini yeye hajui hilo;[i]
Nao wanakuwa wasio
na maana, lakini yeye
hawafikirii.
22 Ila tu nyama yake iliyo
juu yake ndiyo
itakayoendelea kuuma,
Na nafsi yake ikiwa
ingali ndani yake ndiyo
itakayoendelea
kuomboleza."

15 Naye Elifazi Mtemani
akajibu, akasema:
2 "Je, mtu mwenye hekima
atajibu kwa ujuzi wa
upepo,[a]
Au, je, atalijaza tumbo lake
upepo wa mashariki?[b]
3 Kukaripia tu kwa neno
hakutakuwa na faida
yoyote,
Na maneno matupu peke
yake hayatakuwa na
faida.
4 Hata hivyo, wewe
mwenyewe unafanya
woga mbele za Mungu
usiwe na nguvu zozote,
Nawe unapunguza kuwa
na hangaiko lolote mbele
za Mungu.
5 Kwa maana kosa
lako linakizoeza kinywa
chako,
Nawe unachagua ulimi wa
watu werevu.
6 Kinywa chako
kinakutangaza wewe
kuwa mwovu, wala si
mimi;
Na midomo yako
mwenyewe inajibu juu
yako.[c]
7 Je, wewe ndiye
mwanadamu wa kwanza
kabisa kuzaliwa,[d]
Au, je, ulizaliwa kwa
uchungu kabla ya
vilima?[e]
8 Je, wewe husikiliza
mazungumzo ya siri ya
Mungu,[f]
Na je, ni wewe peke yako
mwenye hekima?

SURA 14
a Yoh 11:25
Mdo 26:8
1Ko 15:12
Ufu 20:13
b Ro 8:20
Ebr 11:13
Yak 5:8
c Ayu 19:25
d Da 12:13
Yoh 5:28
Yoh 11:43
e Zb 139:3
Yer 32:19
f Zb 130:3
g Kum 32:35
Ho 13:12
h Ayu 4:20
Mhu 8:8
Isa 57:16
i 1Sa 4:20
Zb 39:6
Mhu 9:6
Isa 63:16

Safu ya 2

SURA 15
a Ayu 42:7
b Ho 12:1
c Ayu 42:8
d Mwa 4:1
e Zb 90:2
Met 8:25
f Ro 11:34
1Ko 2:11

9 Kwa kweli unajua nini
ambacho sisi hatujui?[a]
Unaelewa nini ambacho sisi
hatuna pia?
10 Mwenye kichwa chenye
mvi na mzee pia, wote
wapo pamoja nasi,[b]
Yeye aliye na siku nyingi
kuliko baba yako.
11 Je, faraja za Mungu
hazikutoshi wewe,
Au neno uliloambiwa kwa
upole?
12 Kwa nini yaliyo moyoni
mwako yanakuchukua,
Na kwa nini macho yako
yanawaka?
13 Kwa maana wewe
unaigeuza roho yako
kinyume cha Mungu
mwenyewe,
Nawe umeyatokeza
maneno katika kinywa
chako mwenyewe.
14 Mwanadamu anayeweza
kufa ni nani ndipo awe
safi,[c]
Au ndipo yeyote
aliyezaliwa na
mwanamke awe upande
wa haki?
15 Tazama! Yeye hana imani
na watakatifu wake,[d]
Na mbingu zenyewe kwa
kweli si safi machoni
pake.[e]
16 Sembuse mtu
anayechukiza na aliye
mpotovu,[f]
Mtu anayekunywa ukosefu
wa uadilifu kama maji!
17 Nitakutangazia. Wewe
nisikilize![g]
Nimeona hata jambo hili,
basi acha nilisimulie,
18 Lile ambalo watu
wenye hekima[h] wenyewe
hulisema

SURA 15
a Ayu 13:2
Ayu 16:2
b Ayu 32:6
c 2Nya 6:36
Zb 51:5
d 1Fa 22:20
Met 8:30
Amo 3:7
e Ayu 25:5
Ayu 42:7
f Ayu 4:19
g Ayu 5:27
h Ayu 8:8

Safu ya 2
a 1Th 5:3
b Ayu 18:12
Isa 8:22
Yud 13
c Zb 59:15
Zb 109:10
d Ayu 18:12
e Ro 2:9
f Ayu 16:2
Ayu 42:7

Na ambalo hawakuficha,
hilo likiwa limetoka kwa
baba zao.
19 Wao peke yao walipewa
nchi hiyo,
Wala hakuna mgeni
aliyepita katikati yao.
20 Mwovu anapata mateso
siku zake zote,
Pia hesabu ya miaka
ambayo imewekewa
mwonevu.
21 Sauti ya vitu vyenye
kutia hofu imo masikioni
mwake;
Mporaji huja juu yake
wakati wa amani.[a]
22 Hasadiki kwamba atarudi
kutoka katika giza,[b]
Naye amewekwa kwa ajili
ya upanga.
23 Anapotea njia akitafuta
mkate—uko wapi?[c]
Anajua vema kwamba siku
ya giza[d] iko tayari
mkononi mwake.
24 Taabu na maumivu
huendelea kumtia hofu;[e]
Humshinda nguvu kama
mfalme aliyejitayarisha
kwa ajili ya shambulio.
25 Kwa sababu yeye
ananyoosha mkono wake
juu ya Mungu
mwenyewe,
Naye anajaribu
kujionyesha kuwa mkuu
juu ya Mweza-Yote;[f]
26 Kwa sababu anakimbia juu
yake kwa ugumu wa
shingo,
Na vinundu vizito vya ngao
zake;
27 Kwa sababu yeye kwa
kweli anafunika uso
wake kwa wingi wa
mafuta yake

Naye anaongeza mafuta
juu ya viuno vyake,[a]
28 Anakaa tu katika majiji
ambayo yatafutiliwa
mbali;
Katika nyumba ambamo
watu hawataendelea
kukaa,
Ambazo kwa hakika
zimekusudiwa kuwa
marundo ya mawe.
29 Yeye hatatajirika wala mali
yake haitaongezeka,
Wala hatatandaza mapato
yao juu ya dunia.[b]
30 Yeye hatageuka kutoka
gizani;
Mwali wa moto utakausha
tawi lake,
Naye ateguka kando
kwa mlipuko wa kinywa
chake Yeye.[c]
31 Na asiwe na imani
katika ubatili, akiwa
anapotoshwa,
Kwa maana badala yake
atapata ubatili mtupu;
32 Itatimizwa kabla ya siku
yake.
Na chipukizi lake
halitakuwa na majani
mengi.[d]
33 Atatupa zabibu zake
mbichi kama mzabibu,
Na kutupilia mbali maua
yake kama mzeituni.
34 Kwa maana kusanyiko la
waasi-imani ni tasa,[e]
Na moto wenyewe
utayateketeza mahema
ya rushwa.[f]
35 Taabu inatungwa mimba
na mambo yenye
kudhuru yanazaliwa,[g]
Nalo tumbo lao
hutayarisha
udanganyifu."

SURA 15
a Zb 17:10
b Ayu 20:28
c Ayu 4:9
d Ayu 22:16
e Ayu 8:13
Ayu 16:2
Ayu 42:7
f Ayu 16:3
Ayu 42:8
g Zb 7:14
Isa 59:4
Yak 1:15

Safu ya 2

SURA 16
a Ayu 13:4
Ayu 19:2
Flp 1:17
b Mhu 10:14
c Mt 7:12
Ro 12:15
1Pe 3:8
d Zb 109:25
Mt 27:39
e Ayu 4:3
Met 27:9
Ga 6:1
f Ayu 2:13
g Ayu 7:3
h Ayu 16:19
i Ayu 10:16
j Mdo 7:54

16 Naye Ayubu akajibu,
akasema:
2 "Nimesikia mambo mengi
kama hayo.
Ninyi nyote ni wafariji
wasumbufu![a]
3 Je, kuna mwisho wa
maneno ya upepo?[b]
Au, je, ni nini kinachowatia
uchungu, ndipo mjibu?
4 Mimi mwenyewe pia
naweza kusema kama
ninyi mnavyosema.
Laiti nafsi zenu zingekuwa
mahali ilipo nafsi yangu,
Je, ningeng'aa kwa maneno
juu yenu,[c]
Na je, ningetikisa kichwa
changu juu yenu?[d]
5 Ningewatia ninyi nguvu
kwa maneno ya kinywa
changu,[e]
Na faraja ya midomo yangu
mwenyewe ingetuliza—.
6 Nikiongea, maumivu
yangu mwenyewe
hayatulizwi,[f]
Nami nikiacha kufanya
hivyo, ni nini
kinachoondoka kwangu?
7 Ila tu sasa amenichosha;[g]
Amewafanya ukiwa wale
wote wanaokusanyika
pamoja nami.
8 Pia unanikamata. Ni
ushahidi,[h]
Hivi kwamba kukonda
kwangu kunasimama juu
yangu. Kunashuhudia
usoni pangu.
9 Hasira yake imenirarua
vipande-vipande, naye
anashikilia uadui[i] juu
yangu.
Anasaga meno yake juu
yangu.[j]

Adui yangu mwenyewe
anayanoa macho yake
juu yangu.[a]
10 Wamefungua vinywa vyao
wazi juu yangu,[b]
Wamenipiga mashavu
yangu kwa shutuma,
Wanakusanyika juu yangu
wakiwa hesabu kubwa.[c]
11 Mungu ananitia mikononi
mwa wavulana wadogo,
Naye ananitupa kwa nguvu
mikononi mwa waovu.[d]
12 Nilikuwa nimestarehe,
lakini akanitikisa;[e]
Akanikamata nyuma ya
shingo,
akanivunja-vunja,
Naye ananiweka kuwa
shabaha kwa ajili yake
mwenyewe.
13 Wapiga-mishale[f] wake
wananizunguka;
Anapasua wazi figo[g] zangu
wala haoni huruma;
Anaimwaga nyongo yangu
chini.
14 Anaendelea kunitoboa
kama ukuta kwa kunitia
tundu baada ya tundu;
Anakimbia juu yangu kama
mtu mwenye nguvu.[h]
15 Nimeshona nguo ya gunia[i]
juu ya ngozi yangu,
Nami nimetupa pembe
yangu mavumbini.[j]
16 Uso wangu umekuwa
mwekundu kwa sababu
ya kulia,[k]
Na kuna kivuli kizito juu
ya kope zangu,[l]
17 Ijapokuwa hakuna jeuri
mikononi mwangu,
Na sala yangu ni safi.[m]
18 Ee dunia, usifunike damu[n]
yangu!
Wala pasiwepo mahali kwa
ajili ya kilio changu!

SURA 16
a Ayu 33:10
b Zb 22:13
c Zb 35:15
d Zb 27:12
e Ayu 1:12
Ayu 1:17
f Ayu 7:20
g Zb 73:21
Omb 3:13
h Omb 3:3
i 1Fa 21:27
2Fa 6:30
j Ayu 30:19
Zb 7:5
k Zb 6:6
Zb 31:9
Omb 1:16
l Omb 5:17
m Met 15:8
n Mwa 4:10
Zb 72:14

Safu ya 2
a 1Sa 12:5
Ro 1:9
2Ko 11:31
1Th 2:10
b Ayu 12:4
c Zb 40:1
Zb 142:2
Lu 18:1
d Ayu 31:35
Mhu 6:10
Isa 45:9
Ro 9:20
e Ayu 7:9
Ayu 14:10
Mhu 12:5

SURA 17
f Isa 57:15
g Zb 88:4
Isa 38:10
h Zb 35:16
Ebr 11:36
i 1Sa 25:29
Zb 119:122
j 2Fa 10:15
Met 11:21
Met 17:18
k 2Sa 17:14
Isa 6:10
Mt 11:25
Ro 11:8
l Ayu 11:20
m Ayu 30:9
Zb 69:11

19 Pia sasa, tazama! yeye
anayenishuhudia yuko
mbinguni,
Na shahidi wangu yuko
katika sehemu za juu.[a]
20 Rafiki zangu ni
watu wanaosema kwa
kunipinga;[b]
Jicho langu limemtazama
Mungu bila usingizi.[c]
21 Na uamuzi utafanywa
kati ya mwanamume na
Mungu,
Kama ilivyo kati ya
mwana wa binadamu na
mwenzake.[d]
22 Kwa maana miaka
michache tu itakuja,
Nami nitaenda zangu
kupitia njia ambayo
sitairudia.[e]

17 "Roho yangu imevunjwa,[f]
siku zangu
zimezimwa;
Uwanja wa makaburi ni
kwa ajili yangu.[g]
2 Hakika ninafanyiwa
mzaha,[h]
Na jicho langu linakaa
katikati ya tabia yao ya
uasi.
3 Tafadhali, weka rehani
yangu kwako.[i]
Kuna nani mwingine
atakayenisalimu kwa
mkono[j] kuwa rehani?
4 Kwa maana umefunga
moyo wao usiwe na
busara.[k]
Ndiyo sababu huwainui.
5 Huenda akawaambia rafiki
wachukue mafungu yao,
Lakini macho ya wanawe
yataisha nguvu.[l]
6 Naye ameniweka kuwa
neno la kimethali[m] la
vikundi vya watu,

Hivi kwamba ninakuwa
mtu ambaye uso wake ni
wa kutemewa mate.[a]
7 Na jicho langu linaingia
giza kutokana na
usumbufu[b]
Na viungo vyangu vyote ni
kama kivuli.
8 Watu wanyoofu
wanaangalia kwa
mshangao,
Na hata mtu asiye na hatia
anachacha kwa sababu
ya mwasi-imani.
9 Mwadilifu anaendelea
kuishika sana njia yake,[c]
Na mwenye mikono safi[d]
anaendelea kuongezeka
nguvu.[e]
10 Hata hivyo, ninyi nyote
mnaweza kuanza tena.
Haya, tafadhali,
Kwa kuwa sioni yeyote
mwenye hekima kati
yenu.[f]
11 Siku zangu zimepita,[g]
mipango yangu
imevunjika,[h]
Tamaa za moyo wangu.
12 Wanaendelea kuweka
usiku badala ya mchana:[i]
'Nuru iko karibu kwa
sababu ya giza.'
13 Nikiendelea kungojea,
Kaburi* ndilo nyumba
yangu;[j]
Nitatandika kitanda
changu gizani.[k]
14 Nitalipaazia shimo[l] sauti,
'Wewe ni baba yangu!'
Na kumwambia funza,[m]
'Wewe ni mama yangu na
dada yangu!'
15 Kwa hiyo, basi, liko wapi
tumaini langu?[n]
Na tumaini langu—ni nani
anayeliona?

SURA 17
a Ayu 30:10
b Ayu 16:16
Zb 6:7
Zb 31:9
c Zb 119:165
Met 4:11
d Mwa 20:5
Zb 24:4
Zb 26:6
e Zb 84:7
f Ayu 6:29
Ro 1:22
g Ayu 7:6
Ayu 9:25
Isa 38:10
h Yak 4:13
i Isa 5:20
Yoh 3:19
j Mhu 12:5
Mhu 12:7
k Ayu 10:21
Isa 47:5
l Zb 30:3
Zb 49:9
Zb 143:7
Met 1:12
Isa 14:15
Yon 2:6
m Ayu 24:20
Isa 14:11
Mk 9:48
n Ayu 7:6
Ayu 14:19
Ayu 19:10

Safu ya 2
a Mwa 3:19
Ayu 3:19
Mhu 3:20

SURA 18
b Zb 73:22
2Pe 2:12
c Met 13:9
Met 24:20
d Ayu 21:17
e Ayu 5:13
f Ayu 22:10
g Yer 18:22
h Ayu 5:5
Zb 140:5

16 Watashuka chini kwenye
mapingo ya Kaburi,*
Wakati ambapo sisi,
sote pamoja, tutashuka
mavumbini."[a]

18 Naye Bildadi Mshua aka-
jibu, akasema:
2 "Ninyi mtachukua muda
gani ili kukomesha
maneno?
Mnapaswa kuelewa, ili
baadaye tuseme.
3 Kwa nini tuhesabiwe kuwa
wanyama[b]
Na kuonwa kuwa wasio safi
machoni penu?
4 Yeye anararua
vipande-vipande nafsi
yake katika hasira yake.
Je, dunia iachwe kwa ajili
yako,
Au jiwe liondoke mahali
pake?
5 Pia nuru ya waovu
itazimwa[c]
Na cheche ya moto wake
haitang'aa.
6 Hakika nuru itafifia katika
hema lake,[d]
Na humo taa yake
itazimwa.
7 Hatua zake zenye nguvu
zitasongwa.
Hata shauri lake
litamtupilia mbali.[e]
8 Kwa maana miguu yake
itamwingiza ndani ya
wavu,
Naye atatembea kwenye
kamba za wavu.[f]
9 Mtego utamkamata
kisigino;[g]
Mnaso[h] unaendelea
kumkamata.
10 Kamba imefichwa katika
udongo kwa ajili yake,

Ayu 17:13* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

Ayu 17:16* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

Na kwa ajili yake chombo
cha kunasia katika njia
yake.
11 Pande zote, hofu
za ghafula hakika
zinamshtua kwa woga,[a]
Na kwelikweli kumfukuza
miguuni pake.
12 Nguvu zake zinaliwa na
njaa,
Na msiba[b] husimama
tayari ili kumfanya
achechemee.
13 Utakula vipande vya ngozi
yake;
Mzaliwa wa kwanza wa
kifo atakula viungo
vyake.
14 Uhakika wake
utaondolewa katika
hema lake[c]
Nayo itampeleka kwa
mfalme wa hofu.
15 Ndani ya hema lake
kitakaa kitu ambacho si
chake;
Kiberiti[d] kitatawanywa juu
ya makao yake.
16 Chini, mizizi yake
itakauka,[e]
Na juu, tawi lake
litanyauka.
17 Kutajwa kwake hakika
kutaangamia kutoka
duniani,[f]
Wala hatakuwa na jina
lolote nje barabarani.
18 Watamsukuma kutoka
nuruni kuingia gizani,
Nao watamfukuza kutoka
katika nchi yenye kuzaa.
19 Hatakuwa na wazao wala
watoto katikati ya watu
wake,[g]
Wala hapatakuwa na
mwokokaji mahali pake
pa makao ya kigeni.

SURA 18
a Ayu 15:21
Ayu 20:25
b Ayu 15:23
c Ayu 8:14
Ayu 11:20
d Kum 29:23
e Ayu 29:19
f Met 10:7
g Ayu 42:8

Safu ya 2

SURA 19
a Zb 42:10
b Zb 55:21
Met 12:18
Yak 3:8
c Ayu 6:14
Met 18:24
Mt 7:12
d Ro 3:23
e Zb 38:16
f Zb 69:26
g Zb 66:11
Omb 1:13
h Zb 22:2
Hab 1:2
i Lu 18:7
j Ayu 3:23
Zb 88:8
Omb 3:7

20 Watu walio Magharibi
wataiangalia siku yake
kwa mshangao,
Na hata watu walio
Mashariki watashikwa
na mtetemeko.
21 Ila tu hizo ndizo maskani
za mkosaji,
Na hapa ndipo mahali pa
mtu ambaye hajamjua
Mungu."

19 Naye Ayubu akajibu,
akasema:
2 "Ninyi mtaendelea
kunikasirisha nafsi
yangu mpaka wakati
gani[a]
Na kuendelea kuniponda
kwa maneno?[b]
3 Hizi mara kumi
mmenikemea;
Hamna aibu kwamba
mnanitendea kwa ugumu
hivyo.[c]
4 Na, kama nimefanya kosa,[d]
Hilo kosa litakaa pamoja
nami.
5 Ikiwa kwa kweli
mnajivuna sana juu
yangu,[e]
Na kuonyesha kwamba
shutuma yangu inanifaa,[f]
6 Jueni, basi, kwamba
Mungu mwenyewe
amenipotosha,
Naye ameuzungusha wavu
wake wa kuwindia juu
yangu.[g]
7 Tazama! Ninaendelea
kupaaza sauti, 'Jeuri!'
lakini sipati jibu lolote;[h]
Naendelea kulia nipewe
msaada, lakini hakuna
haki.[i]
8 Amezuia pito langu kwa
ukuta wa mawe,[j] nami
siwezi kupita;

Naye anaweka giza katika
barabara zangu.[a]
9 Amenivua utukufu
wangu,[b]
Naye anaondoa taji la
kichwa changu.
10 Ananibomoa pande zote,
nami naenda zangu;
Naye anang'oa tumaini
langu kama mti.
11 Pia hasira yake inawaka
juu yangu,[c]
Naye anaendelea
kunihesabu kuwa adui
yake.
12 Vikosi vyake vinakuja kwa
muungano na kujenga
njia yao juu yangu,[d]
Nao wanapiga kambi
kuzunguka hema langu.
13 Ndugu zangu amewaweka
mbali sana nami,[e]
Na wale wanaonijua hata
wamejitenga nami.
14 Watu ninaofahamiana nao
wamekoma kuwapo,[f]
Na wale ninaowajua
wamenisahau,
15 Wale wanaokaa wakiwa
wageni nyumbani
mwangu;[g] na vijakazi
wangu wananiona kuwa
mgeni;
Nimekuwa mgeni
kwelikweli machoni pao.
16 Nimemwita mtumishi
wangu, lakini hajibu.
Ninaendelea kumwomba
huruma kwa kinywa
changu mwenyewe.
17 Pumzi yangu imemchukiza
mke wangu,[h]
Nami nimenuka kwa wana
wa tumbo la mama
yangu.
18 Pia wavulana wadogo
wenyewe wamenikataa;[i]

SURA 19

a Isa 50:10
Yer 13:16
b Zb 89:44
c Ayu 13:24
d Ayu 30:12
e Zb 31:11
Zb 38:11
Zb 69:8
f Zb 38:11
g Ayu 31:32
h Ayu 2:9
i 2Fa 2:23

Safu ya 2

a Ayu 17:6
Zb 88:8
b Zb 109:5
c Ayu 30:30
Ayu 33:21
Zb 102:5
Omb 4:8
d Mt 5:7
1Pe 3:8
e Ayu 1:11
Zb 38:2
f Ayu 2:10
Zb 69:26
g Yer 17:1
h Ayu 14:14
Zb 19:14
Zb 69:18
Zb 103:4
Met 23:11
Mt 20:28
i Mk 10:45
Ro 3:24
1Ko 1:30

Ninaposimama tu,
wanaanza kunisema.
19 Watu wote wa kikundi
cha rafiki zangu
wananichukia,[a]
Na wale ambao
nimewapenda
wamenigeuka.[b]
20 Mifupa yangu
inashikamana na ngozi
na nyama yangu,[c]
Nami ninaponyoka na
ngozi ya meno yangu.
21 Mnionyeshe kibali kidogo,
mnionyeshe kibali
kidogo, enyi rafiki
zangu,[d]
Kwa kuwa mkono
wenyewe wa Mungu
umenigusa.[e]
22 Kwa nini mnaendelea
kunitesa kama
anavyofanya Mungu,[f]
Na hamshibi nyama yangu?
23 Laiti sasa maneno yangu
yangekuwa
yameandikwa!
Laiti yangekuwa
yameandikwa katika
kitabu!
24 Kwa kalamu ya chuma[g] na
kwa risasi,
Laiti yangekuwa
yamechongwa milele
katika mwamba!
25 Nami mwenyewe najua
vema kwamba mkombozi
wangu[h] yuko hai,
Na kwamba, akija baada
yangu, yeye atasimama[i]
juu ya mavumbi.
26 Na baada ya ngozi
yangu, ambayo
wameichuna,—hii!
Lakini ijapokuwa
kupungua kwa mwili
wangu nitamwona
Mungu,

27 Ambaye mimi mwenyewe nitamwona,[a]
Na ambaye macho yangu hakika yatamwona, bali si mgeni.
Figo zangu zimeisha nguvu ndani yangu kabisa.
28 Kwa maana ninyi mnasema, ‘Kwa nini tunaendelea kumtesa?’[b]
Wakati mzizi wenyewe wa jambo hili unapatikana ndani yangu.
29 Ogopeni kwa ajili yenu kwa sababu ya upanga,[c]
Kwa kuwa upanga unamaanisha ghadhabu juu ya makosa,
Ili ninyi mjue kwamba kuna mwamuzi.”[d]

20 Naye Sofari Mnaamathi akajibu, akasema:
2 “Ni kwa sababu hiyo fikira zangu zinazonifadhaisha zinanijibu,
Kwa sababu ya wasiwasi wangu wa ndani.
3 Nasikia himizo ambalo linanitusi;
Na roho ambayo haina uelewaji nilio nao mimi inanijibu.
4 Je, nyakati zote umelijua jambo hili,
Tangu mwanadamu alipowekwa duniani,[e]
5 Kwamba kilio cha shangwe cha watu waovu ni kifupi[f]
Na kushangilia kwa mwasi-imani ni kwa kitambo kidogo?
6 Ijapokuwa utukufu wake unapaa mbinguni[g]
Na kichwa chake chenyewe kinafika mawinguni,
7 Yeye anaangamia milele kama mavi yake;[h]
Wale wanaomwona watasema, ‘Yeye yuko wapi?’[a]
8 Ataruka mbali kama ndoto, nao hawatampata;
Naye atafukuziwa mbali kama maono ya usiku.[b]
9 Jicho ambalo limemwona halitafanya hivyo tena,[c]
Na mahali pake hapatamwona tena.[d]
10 Wanawe watatafuta kibali cha watu wa hali ya chini,
Na mikono yake mwenyewe itarudisha vitu vyake vyenye thamani.[e]
11 Mifupa yake imekuwa yenye kujaa nguvu yake ya ujana,
Lakini italala pamoja naye katika mavumbi matupu.[f]
12 Ikiwa kilicho kibaya kina ladha tamu kinywani mwake,
Ikiwa anakiyeyusha chini ya ulimi wake,
13 Ikiwa anakihurumia wala hakiachi,
Na ikiwa anaendelea kukizuia katikati ya kaakaa lake,
14 Chakula chake hakika kitabadilishwa katika matumbo yake;
Kitakuwa nyongo ya swila ndani yake.
15 Amemeza mali, lakini ataitapika;
Mungu ataiondosha tumboni mwake.
16 Atanyonya sumu ya swila;
Ulimi wa nyoka utamuua.[g]
17 Hataiona kamwe mifereji ya maji,[h]
Vijito vya asali na siagi.

SURA 19
a Zb 17:15
b Zb 69:26
c Kum 32:41
d Zb 58:11; Mt 7:1; Ro 14:4; Yak 4:12

SURA 20
e Mwa 1:27; Ayu 8:8
f Zb 37:36
g Isa 14:13; Amo 9:2; Oba 4
h Zb 83:10; Yer 8:2

Safu ya 2
a Ayu 14:10
b Zb 73:20; Zb 90:5
c Zb 37:36
d Ayu 8:18; Zb 103:16
e Ayu 20:18
f Ayu 21:26
g Kum 32:33
h Zb 36:9; Yer 17:6

18 Atairudisha mali yake
aliyojipatia wala
hataimeza;
Kama mali kutokana na
biashara yake, lakini
ambayo hataifurahia.[a]
19 Kwa maana ameponda
vipande-vipande,
amewaacha watu wa hali
ya chini;
Ameinyakua nyumba
ambayo hakuijenga.[b]
20 Kwa maana hakika hatajua
starehe katika tumbo
lake;
Hataponyoka kupitia
vitu vyake vyenye
kutamanika.[c]
21 Hakuna chochote
kilichobaki kwa ajili
yake ili kumeza;
Ndiyo sababu hali njema
yake haitadumu.
22 Atakuwa na mahangaiko
wakati wingi wake
umefikia kilele;[d]
Nguvu zote za maafa
zitakuja juu yake.
23 Na iwe kwamba, ili kujaza
tumbo lake,
Ataipeleka hasira yake
inayowaka juu yake[e]
Naye atainyesha juu yake,
ndani ya matumbo yake.
24 Ataikimbia[f] silaha ya
chuma;
Upinde wa shaba
utamkatakata.
25 Mshale utachomoka
kupitia mgongo wake,
Na silaha inayong'aa
kupitia nyongo yake;[g]
Vitu vyenye kuogopesha
vitaenda juu yake.[h]
26 Giza lote litawekwa akiba
kwa ajili ya hazina zake;

SURA 20
a Ayu 20:10
b Ayu 35:9
c Met 11:4
Mhu 5:13
d Mhu 5:12
e Hes 11:33
Zb 78:31
f Isa 24:18
Amo 9:2
g Ayu 16:13
h Ayu 18:11

Safu ya 2
a Zb 21:9
b Zb 44:21
Mal 3:5
c Zb 11:6
d Ayu 27:13
Ayu 31:3
Met 10:7

SURA 21
e Ayu 16:10
Ayu 16:20
Ayu 17:2
Ebr 11:36
f Amu 18:19
Ayu 40:4
Met 30:32
g Isa 55:7
Eze 33:11
Hab 1:3
Hab 1:13
Ro 9:17
Ro 9:22

Moto ambao hakuna mtu
aliyeupepea
utamteketeza;[a]
Mambo yatamwendea
vibaya mwenye kuokoka
aliye katika hema lake.
27 Mbingu itafunua kosa
lake,[b]
Na dunia itafanya maasi
juu yake.
28 Mvua kubwa itaifagilia
mbali nyumba yake;
Kutakuwa na vitu
vilivyomwagwa katika
siku ya hasira yake.[c]
29 Hilo ndilo fungu la
mtu mwovu kutoka kwa
Mungu,[d]
Urithi wake uliosemwa
kutoka kwa Mungu."

21 Naye Ayubu akajibu,
akasema:
2 "Sikilizeni neno langu kwa
makini,
Na hili liwe faraja yenu.
3 Mnivumilie, nami
nitasema;
Na baada ya mimi
kusema kila mmoja wenu
anaweza kudhihaki.[e]
4 Kwa habari yangu,
je, hangaiko langu
linaelekezwa kwa
mwanadamu?
Au ni kwa nini roho yangu
haikosi subira?
5 Geuzeni nyuso zenu
kunielekea na kuangalia
kwa mshangao,
Na mweke mkono wenu juu
ya kinywa chenu.[f]
6 Na ikiwa nimekumbuka,
pia nimetiwa wasiwasi,
Na mtetemeko umeushika
mwili wangu.
7 Kwa nini waovu
wanaendelea kuishi,[g]

Wamezeeka, pia
wamekuwa na mali
nyingi zaidi?[a]
8 Uzao wao umefanywa
imara nao machoni pao,
Na wazao wao mbele ya
macho yao.
9 Nyumba zao ni amani, bila
hofu,[b]
Na fimbo ya Mungu haiko
juu yao.
10 Ng'ombe-dume wake kwa
kweli hutia mimba, wala
hapotezi shahawa;
Ng'ombe wake huzaa[c] wala
hatokwi na mimba.
11 Wanaendelea kuwatuma
wavulana wao wadogo
kama kundi,
Na watoto wao wa kiume
wanaruka huku na huku.
12 Wao wanaendelea kupaaza
sauti yao kwa tari na
kinubi,[d]
Nao huendelea kushangilia
sauti ya zumari.
13 Wao hutumia siku zao
katika starehe,[e]
Nao baada ya kitambo
kidogo wanashuka
mpaka katika Kaburi.*
14 Nao wanamwambia Mungu
wa kweli, 'Tuondokee![f]
Nasi hatujaona upendezi
wowote katika kuzijua
njia zako.[g]
15 Mweza-Yote ana thamani
gani, ndipo tumtumikie,[h]
Nasi tunajifaidi jinsi gani
kwa kuwa tumewasiliana
naye?'[i]
16 Tazama! Hali njema yao
haiko katika nguvu zao
wenyewe.[j]
Shauri la waovu limekaa
mbali nami.[k]

Ayu 21:13* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

SURA 21

a Ayu 12:6
Zb 37:7
Zb 73:3
Zb 73:12
Yer 12:1
b Zb 73:5
c Zb 144:14
d Isa 5:12
Isa 22:13
Amo 6:5
e Mt 24:38
Lu 12:20
Lu 17:28
1Ko 15:32
f Ayu 22:17
Zb 10:11
Zb 73:11
g Yoh 3:19
Ro 1:28
h Kut 5:2
Zb 10:4
Ho 13:6
i Ayu 34:9
Ayu 35:3
Mal 3:14
j Zb 49:7
Mhu 8:8
k Ayu 22:18
Zb 1:1

Safu ya 2

a Met 20:20
Met 24:20
b Zb 73:19
Lu 12:46
c Kut 15:7
Zb 1:4
Zb 35:5
Isa 17:13
Ho 13:3
Mt 3:12
d Kut 20:5
e Zb 11:6
Isa 26:11
f Zb 75:8
Isa 51:17
Yer 25:15
Ufu 14:10
g Zb 55:23
h Isa 40:14
Ro 11:34
1Ko 2:16
i Isa 40:23
2Pe 2:4
Yud 9
j Zb 49:17
Lu 12:20

17 Taa ya waovu inazimwa
mara ngapi,[a]
Na msiba wao unakuja juu
yao mara ngapi?
Ni mara ngapi yeye
anagawanya maangamizi
katika hasira yake?[b]
18 Je, wao wanakuwa kama
nyasi mbele ya upepo,[c]
Na kama makapi ambayo
dhoruba imepeperushia
mbali?
19 Mungu mwenyewe ataweka
akiba ya madhara ya mtu
kwa ajili ya wana wa mtu
huyo;[d]
Atampa thawabu ili ajue
hayo.[e]
20 Macho yake yataona
kudhoofika kwake,
Naye atakunywa kutokana
na ghadhabu ya
Mweza-Yote.[f]
21 Je, kupendezwa kwake
kutakuwa nini katika
nyumba yake baada
yake,
Wakati hesabu ya miezi
yake itakapokatwa mara
mbili?[g]
22 Je, atamfundisha hata
Mungu ujuzi,[h]
Wakati yeye Huyo
anawahukumu walio
juu?[i]
23 Yeye mwenyewe atakufa
wakati amejitosheleza
kwa ukamili,[j]
Anapokuwa bila
mahangaiko kabisa na
akiwa amestarehe;
24 Wakati mapaja yake
mwenyewe yamejaa
mafuta
Na urojorojo wa mifupa
yake unawekwa ukiwa na
umajimaji.

25 Na huyu mwingine atakufa
akiwa na nafsi yenye
uchungu
Wakati hajala vitu vyema.[a]
26 Watalala pamoja
mavumbini[b]
Na funza watawafunika.[c]
27 Tazama! Najua vema fikira
zenu
Na hila ambazo mnataka
kunitendea kijeuri.[d]
28 Kwa maana mnasema, 'Iko
wapi nyumba ya mtu
mwenye cheo,
Na liko wapi hema,
maskani za waovu?'[e]
29 Je, hamjawauliza wale
wanaosafiri barabarani?
Na je, hamkagui kwa
uangalifu ishara zao,
30 Kwamba katika siku ya
msiba mwovu huachwa,[f]
Katika siku ya ghadhabu
yeye hukombolewa?
31 Ni nani atakayemwambia
juu ya njia yake usoni
pake?[g]
Na ni nani atakayempa
thawabu kwa ajili ya yale
ambayo yeye mwenyewe
amefanya?[h]
32 Naye ataletwa kwenye
uwanja wa makaburi,[i]
Na kukesha kutafanywa
kwenye kaburi.
33 Kwake yeye madonge
ya udongo wa bonde la
mto hakika yatakuwa
matamu,[j]
Naye atavuta wanadamu
wote nyuma yake,[k]
Na wale waliokuwa mbele
yake hawakuwa na
hesabu.
34 Kwa hiyo ni kwa ubatili
jinsi mnavyojaribu
kunifariji,[l]
Na majibu yenu yanabaki
kuwa ukosefu wa
uaminifu!"

22 Naye Elifazi Mtemani
akajibu, akasema:
2 "Je, mwanamume anaweza
kuwa na faida kwa
Mungu mwenyewe,[a]
Kwamba mtu mwenye
ufahamu awe na faida
kwake?
3 Je, Mweza-Yote
anapendezwa kwa
vyovyote kwa kuwa
wewe ni mwadilifu,[b]
Au, kupata faida yoyote
kwa kuwa wewe
unafanya njia yako isiwe
na lawama?[c]
4 Je, atakukaripia wewe kwa
sababu ya kumheshimu,
Je, ataingia hukumuni
pamoja nawe?[d]
5 Je, tayari ubaya wako
mwenyewe si mwingi
sana,[e]
Na je, hakuna mwisho wa
makosa yako?
6 Kwa maana wewe
unanyakua rehani
kutoka kwa ndugu zako
bila sababu,[f]
Nawe unavua hata mavazi
ya watu walio uchi.
7 Humpi mwenye kuchoka
maji ya kunywa,
Nawe unamnyima mwenye
njaa mkate.[g]
8 Na kwa habari ya mtu
mwenye nguvu, nchi ni
yake,[h]
Na mtu anayetendewa kwa
upendeleo anakaa humo.
9 Umewafukuza wajane
wakiwa mikono mitupu,
Na mikono ya wavulana
wasio na baba
imepondwa.[i]

SURA 21
a 1Fa 17:12
Met 13:21
b Ayu 3:19
Mhu 3:20
Mhu 9:2
c Ayu 24:20
Isa 14:11
d Zb 59:3
e Ayu 20:7
f Met 16:4
2Pe 2:9
g Ga 2:11
h Isa 59:18
Ro 12:19
i Ayu 17:16
j Ayu 3:17
k Ro 5:12
l Ayu 16:2

Safu ya 2

SURA 22
a Kut 3:10
Ayu 42:8
2Ko 5:20
b Met 15:8
Yer 9:24
c Ayu 2:3
Met 11:20
Met 27:11
d Zb 7:9
e Ayu 1:8
Ayu 4:7
f Ayu 31:19
Ayu 42:7
g Ayu 31:17
Ayu 42:8
h Ayu 31:25
i Ayu 42:7
Met 29:12
Met 31:21

10 Ndiyo sababu mitego
ya ndege imekuzunguka
pande zote,[a]
Na hofu ya ghafula
inakutia wasiwasi;
11 Au giza, hivi kwamba
huwezi kuona,
Na mkusanyo wa maji
yanayosukasuka
unakufunika.
12 Je, Mungu hayuko juu
kama mbingu?[b]
Pia ona jumla ya hesabu ya
nyota,[c] kwamba ziko juu.
13 Na bado umesema: 'Kweli
Mungu anajua nini?
Je, anaweza kuhukumu
kupitia giza zito?
14 Mawingu ni mahali pake
pa kujificha hivi kwamba
haoni,
Naye hutembea huku na
huku juu ya ngome ya
mbingu.'
15 Je, utaendelea kuifuata
njia ya zamani za kale
Ambayo watu wenye
kudhuru wametembea,
16 Watu ambao
wamenyakuliwa kabla ya
wakati wao,[d]
Ambao msingi[e] wao
unamwagwa kama mto,
17 Ambao wanamwambia
Mungu wa kweli:
'Tuondokee![f]
Na Mweza-Yote anaweza
kutimiza nini juu yetu?'
18 Na hali yeye mwenyewe
amezijaza nyumba zao
vitu vyema;[g]
Na shauri la waovu limekaa
mbali nami.[h]
19 Waadilifu wataona na
kushangilia,[i]
Na asiye na hatia
atawadhihaki:

SURA 22
a Ayu 18:9
b Zb 115:3
c Zb 147:4
d Zb 55:23
e Ayu 4:19
f Isa 30:11
g Zb 17:14
Mt 5:45
Mdo 14:17
h Ayu 21:16
i Zb 107:42

Safu ya 2
a Ayu 11:13
b Ayu 8:5
c 1Fa 9:28
Ayu 28:16
Zb 45:9
Isa 13:12
d Isa 33:6
e Zb 37:4
f Ayu 27:10
g Zb 65:2
h Zb 116:14
Mhu 5:4
i Met 4:18
j Met 16:18
Met 29:23
Yak 4:6
1Pe 5:5
k Zb 138:6
Isa 66:2
Lu 18:13

20 'Kwa kweli wapinzani wetu
wamefutiliwa mbali;
Na mabaki yao hakika
moto utayateketeza.'
21 Tafadhali, fahamiana naye,
na udumishe amani;
Hivyo mambo mema
yatakujia.
22 Tafadhali, chukua sheria
kutoka kinywani mwake,
Na utie maneno yake
moyoni mwako.[a]
23 Ukirudi kwa Mweza-Yote,[b]
utajengwa;
Ukiweka ukosefu wa
uadilifu mbali na hema
lako,
24 Na mawe ya madini yenye
thamani yakiwekwa
katika mavumbi
Na dhahabu ya Ofiri[c]
katika mwamba wa
mabonde ya mito,
25 Pia Mweza-Yote kwelikweli
atakuwa madini yako
yenye thamani,
Na fedha, iliyo bora kabisa,
kwako.[d]
26 Kwa maana ndipo
utakapopata furaha tele
katika Mweza-Yote,[e]
Nawe utamwinulia Mungu
mwenyewe uso wako.[f]
27 Utamsihi, naye
atakusikiliza;[g]
Nawe utazitimiza nadhiri
zako.[h]
28 Nawe utafanya uamuzi
kuhusu jambo fulani,
nalo litasimama kwako;
Na hakika nuru
itaziangaza njia zako.[i]
29 Kwa maana lazima
itakuwepo fedheha
unaposema kwa kiburi;[j]
Lakini yeye atamwokoa
mtu mwenye macho ya
unyenyekevu.[k]

30 Atamwokoa mtu asiye na hatia,[a]
Nawe hakika utaokolewa kwa ajili ya usafi wa mikono yako.”[b]

23 Naye Ayubu akajibu, akasema:

2 “Hata leo hangaiko[c] langu ni uasi;
Mkono wangu wenyewe ni mzito kwa sababu ya kuugua kwangu.
3 Laiti ningejua kweli mahali ambapo ningeweza kumpata![d]
Ningeenda mpaka mahali pake pa kudumu.[e]
4 Ningeleta mbele zake kesi ya hukumu,
Nami ningekijaza kinywa changu na hoja za kujibu;
5 Ningeyajua maneno anayonijibu,
Nami ningefikiria yale anayoniambia.[f]
6 Je, yeye angeshindana nami kwa wingi wa nguvu?
Hapana! Hakika yeye angenisikiliza mimi.[g]
7 Hapo mtu mnyoofu mwenyewe atanyoosha mambo pamoja na yeye,
Nami ningeenda nikiwa salama milele kutoka kwa mwamuzi wangu.
8 Tazama! Ninaenda upande wa mashariki, naye hayuko huko;
Na kurudi tena, nami siwezi kumtambua;[h]
9 Kuelekea upande wa kushoto ambako anafanya kazi, lakini siwezi kumwona;
Anageuka kando upande wa kuume, lakini simwoni.
10 Kwa maana yeye anajua vema ile njia ninayoenda.[a]
Baada ya yeye kunijaribu, nitatoka nikiwa kama dhahabu.[b]
11 Mguu wangu umezishika hatua zake;
Njia yake nimeishika, wala sigeuki kando.[c]
12 Siondoki katika amri ya midomo yake.[d]
Nimeyachukua kuwa hazina maneno ya kinywa chake[e] kuliko yale niliyoamriwa.
13 Naye ana akili moja, na ni nani anayeweza kumpinga?[f]
Na nafsi yake mwenyewe ina tamaa, naye ataifanya.[g]
14 Kwa maana atatenda kikamilifu yale niliyoamriwa,[h]
Na mambo kama hayo ni mengi kwake.
15 Ndiyo maana nimeingiwa na wasiwasi kwa sababu yake;
Nimekaza fikira nami ninamhofu.[i]
16 Hata Mungu mwenyewe ameutia moyo wangu woga,[j]
Na Mweza-Yote mwenyewe amenitia wasiwasi.[k]
17 Kwa maana sikunyamazishwa kimya kwa sababu ya giza,
Wala kwa sababu weusi umeufunika uso wangu.

24 “Kwa nini nyakati hazijawekwa akiba na Mweza-Yote,[l]
Na wale wanaomjua hawajaziona siku zake?[m]

SURA 22
a Mwa 19:16; 2Pe 2:9
b Zb 24:4

SURA 23
c Ayu 10:1
d Ayu 13:3; Ayu 16:21
e Ayu 31:37
f Zb 49:3
g Zb 22:24; Isa 57:16
h Ayu 9:11

Safu ya 2
a Ayu 1:8; Zb 1:6; Zb 139:1
b Ayu 31:6; Zb 17:3; 1Pe 1:7
c Zb 18:21; Zb 44:18
d 1Yo 5:3
e Zb 119:11; Zb 119:127; Yer 15:16
f Hes 23:19; Hes 23:20; Ro 9:19
g Zb 135:6; Isa 14:24; Isa 46:10
h 1Th 3:3
i Zb 111:10; Zb 119:120; Met 16:6
j Zb 22:14
k Ru 1:20

SURA 24
l Mdo 1:7
m Isa 26:10

2 Kuna wale wanaosogeza
nyuma alama za
mipaka;[a]
Wamenyakua kundi, ili
walichunge.
3 Wanamchukua hata
punda-dume wa
wavulana wasio na baba;
Wanamkamata ng'ombe wa
mjane kuwa rehani.[b]
4 Wanamgeuza kando
maskini aiache njia;[c]
Na wakati uleule wenye
kuteseka wa dunia
wamejificha.
5 Tazama! kama punda-milia[d]
nyikani
Wameenda katika utendaji
wao, kutafuta chakula.
Nchi tambarare ya
jangwani inampa kila
mmoja mkate kwa ajili ya
wavulana.
6 Wanavuna chakula chake
shambani,
Nao wanapora haraka
shamba la mizabibu la
mwovu.
7 Wanakaa uchi usiku kucha
bila vazi,[e]
Na bila chochote cha
kujifunika katika baridi.[f]
8 Wanalowana maji
kutokana na dhoruba ya
mvua ya milimani,
Na kwa sababu hakuna
mahali pa kujikinga[g]
wanalazimika
kuukumbatia mwamba.
9 Wanamnyakua mvulana
asiye na baba hata
kutoka kwenye maziwa,[h]
Nao wanachukua kuwa
rehani kile alicho nacho
mwenye kuteseka.[i]
10 Wanalazimika kutembea
uchi wakiwa bila vazi,
Nao wanalazimika kubeba
masuke yaliyovunwa
wakiwa na njaa.[a]
11 Wanashinda katikati ya
mchana wakiwa kati ya
ukuta wa matuta;
Wanalazimika kukanyaga
mashinikizo ya divai, na
bado wanakuwa na kiu.[b]
12 Kutoka katika jiji
wanaokufa wanaendelea
kuugua,
Na nafsi ya waliotiwa
majeraha ya kufisha
inalia ipewe msaada;[c]
Naye Mungu huona hilo
kuwa si jambo lisilofaa.[d]
13 Kwa habari yao, wakawa
katikati ya wale
wanaoiasi nuru;[e]
Hawakuzitambua njia
zake,
Wala hawakukaa katika
barabara zake.
14 Muuaji anasimama wakati
wa mchana,
Anamuua mwenye
kuteseka na maskini;[f]
Na wakati wa usiku yeye
huwa mwizi wa kawaida.[g]
15 Kwa habari ya jicho la
mzinzi,[h] limengojea giza
la jioni,[i]
Likisema, 'Hakuna jicho
litakaloniona!'[j]
Naye hufunika uso wake.
16 Ametoboa shimo kuingia
katika nyumba wakati
wa giza;
Wakati wa mchana
wanajifungia.
Hawajui nuru ya mchana.[k]
17 Kwa maana kwao asubuhi
ni kama kivuli[l] kizito,
Kwa maana wanazitambua
hofu za ghafula za kivuli
kizito.

SURA 24
a Kum 19:14
Kum 27:17
Met 23:10
Ho 5:10
b Kum 24:17
c Zb 109:16
Met 22:16
Isa 10:2
Amo 8:4
Yak 5:4
d Zb 104:11
Yer 14:6
Isa 32:14
e Kut 22:27
Kum 24:13
f 2Ko 11:27
g Omb 4:5
h 2Fa 4:1
i Kut 22:26
Kum 24:13
Eze 18:12

Safu ya 2
a 1Ti 5:18
b Yer 22:13
Yak 5:4
c Mhu 4:1
d Mhu 8:13
2Pe 3:15
e Yoh 3:19
f Zb 10:8
g Mt 24:43
1Th 5:2
h 2Pe 2:14
i Met 7:9
j 2Sa 12:12
Zb 94:7
Met 30:20
k Yoh 3:20
l Ayu 10:21
Ayu 38:17

18 Yeye ni mwepesi juu ya uso
wa maji.
Mashamba yao yatalaaniwa
duniani.[a]
Hatageuka kuelekea njia
ya mashamba ya
mizabibu.
19 Ukame, pia joto, hunyakua
maji ya theluji;
Nalo Kaburi* wale ambao
wametenda dhambi![b]
20 Tumbo la uzazi litamsahau,
funza atamnyonya kwa
utamu,[c]
Yeye hatakumbukwa tena.[d]
Na ukosefu wa uadilifu
utavunjwa kama mti.[e]
21 Anashughulika pamoja na
mwanamke tasa ambaye
hazai,
Na pamoja na mjane,[f]
ambaye yeye hamtendei
wema wowote.
22 Naye hakika atawavuta
watu wenye nguvu kwa
uwezo wake;
Yeye atasimama asiwe na
uhakika juu ya maisha
yake.
23 Yeye atamfanya awe na
uhakika ili ajitegemeze;[g]
Na macho yake yatakuwa
juu ya njia zao.[h]
24 Wamekuwa huko juu kwa
muda kidogo, kisha
hawako tena,[i]
Nao wameshushwa chini;[j]
wanang'olewa kama kila
mtu mwingine,
Na kama suke la nafaka
wanakatwa.
25 Basi kwa kweli sasa,
ni nani atakayetoa
uhakikisho kuwa mimi
ni mwongo
Au kulifanya neno langu
kuwa si kitu?"

Ayu 24:19* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

SURA 24
a Kum 28:16
Ayu 21:17
Met 3:33
b Zb 49:14
Zb 55:15
Lu 12:20
c Ayu 17:14
Isa 14:11
d Met 10:7
Mhu 8:10
Mhu 9:5
e Mt 3:10
f Kut 22:22
Zek 7:10
g Mhu 8:11
Isa 56:12
Lu 12:19
h Zb 11:4
Met 5:21
Met 15:3
i Zb 37:10
Zb 92:7
Mhu 8:12
Yak 1:11
j Mhu 8:13

Safu ya 2

SURA 25
a Ayu 8:1
Ayu 18:1
b Da 4:3
c Ayu 4:17
d Ayu 15:14
e Zb 22:6

SURA 26
f Ayu 16:2
g Ayu 12:2
Ayu 15:8
Ayu 17:10
h Zb 104:25

25 Naye Bildadi[a] Mshua
akajibu, akasema:
2 "Utawala na hofu ziko
kwake;[b]
Anafanya amani katika
vilele vyake.
3 Je, majeshi yake yana
hesabu?
Na ni juu ya nani nuru yake
haiangazi?
4 Basi mwanadamu
anayeweza kufa
anawezaje kuwa upande
wa haki mbele za
Mungu,[c]
Au, mtu aliyezaliwa
na mwanamke anawezaje
kuwa safi?[d]
5 Tazama! Kuna hata mwezi,
nao si mwangavu;
Nazo nyota zenyewe si safi
machoni pake.
6 Sembuse mwanadamu
anayeweza kufa, ambaye
ni funza,
Na mwana wa binadamu,
ambaye ni mnyoo!"[e]

26 Naye Ayubu akajibu,
akasema:
2 "Lo! Jinsi umekuwa
msaada kwa mtu asiye
na uwezo!
Lo! Jinsi umeokoa mkono
usio na nguvu![f]
3 Jinsi umemshauri mtu
asiye na hekima,[g]
Nawe umefanya umati ujue
hekima inayotumika!
4 Umemwambia nani
maneno,
Na ni pumzi ya nani
imetoka kwako?
5 Wale wasiojiweza katika
kifo wanaendelea
kutetemeka
Chini ya maji na wale
wanaokaa ndani yake.[h]

6 Kaburi* liko uchi mbele zake,[a]
Na mahali pa maangamizi hapana kifuniko.
7 Anaitandaza kaskazini juu ya mahali pasipo na kitu,[b]
Akiitundika dunia pasipo na kitu;
8 Anafunga maji katika mawingu yake,[c]
Hivi kwamba wingu kubwa halipasuki chini yayo;
9 Anaufunika uso wa kiti cha ufalme,
Anatandaza juu yake wingu lake.[d]
10 Amechora mviringo juu ya uso wa maji,[e]
Mpaka mahali ambapo nuru huishia katika giza.
11 Nguzo za mbingu hutikisika,
Nazo hushangaa kwa sababu ya kemeo lake.
12 Kwa uwezo wake ameichochea bahari,[f]
Naye kwa uelewaji wake amemvunja vipande-vipande[g] yule mshambuliaji.[h]
13 Kwa upepo wake ameng'arisha mbingu,[i]
Mkono wake umemchoma yule nyoka anayenyiririka.[j]
14 Tazama! Hizo ndizo kingo za njia zake,[k]
Nao ni mnong'ono ulioje wa jambo lililosikiwa juu yake!
Lakini kuhusu mngurumo wake wenye nguvu ni nani anayeweza kuonyesha uelewaji?"[l]

Ayu 26:6* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

SURA 26
a Zb 139:8; Ebr 4:13
b Ayu 9:8; Zb 104:2; Isa 42:5
c Met 30:4; Mhu 11:3
d Kut 34:5; Zb 97:2
e Met 8:27; Isa 40:22; Yer 5:22
f Zb 74:13; Isa 51:15
g Zb 72:4; Isa 2:12; Da 2:35
h Ayu 9:13
i Zb 33:6; Zb 104:30
j Zb 74:13; Isa 27:1; Isa 51:9
k Zb 65:4; Zb 92:5; Mhu 3:11; Isa 55:9
l Ayu 37:5

Safu ya 2

SURA 27
a Zb 49:4; Zb 78:2
b Kum 6:13; Kum 10:20; Yer 12:16; Ebr 6:16
c Ayu 34:5
d Ru 1:20; 2Fa 4:27
e Mwa 2:7; Isa 42:5; Mdo 17:25
f Kum 25:1; Ayu 40:8; Met 17:15
g Ayu 22:1; Ayu 22:5; Met 27:11; Mt 24:9; Ufu 2:10; Ufu 6:11
h Ayu 2:3
i Mdo 24:16
j 1Sa 25:26
k Ayu 13:16; Ayu 36:13; Ebr 6:6
l Lu 12:20
m Ayu 35:12; Zb 18:41; Met 28:9; Yer 11:11; Yak 4:3

27 Naye Ayubu akatokeza tena neno lake la kimethali,[a] akaendelea kusema:
2 "Kama Mungu anavyoishi,[b] ambaye ameiondoa hukumu yangu,[c]
Na kama Mweza-Yote anavyoishi, ambaye ameitia uchungu nafsi yangu,[d]
3 Pumzi yangu ikiwa bado ni nzima ndani yangu,
Na roho ya Mungu imo ndani ya mianzi ya pua yangu,[e]
4 Midomo yangu haitasema ukosefu wa uadilifu
Wala ulimi wangu hautatamka udanganyifu!
5 Ni jambo lisilowaziwa kwangu kwamba niwatangaze ninyi kuwa waadilifu![f]
Mpaka nitakapokata pumzi, sitajiondolea utimilifu[g] wangu!
6 Nimeishikilia haki yangu, nami sitaiachilia;[h]
Moyo wangu hautanidhihaki kwa ajili ya yoyote ya siku zangu.[i]
7 Adui yangu na awe mwovu katika kila njia,[j]
Na yule anayeniasi awe mkosaji kwelikweli.
8 Kwa maana ni nini tumaini la mwasi-imani iwapo anamkatilia mbali,[k]
Iwapo Mungu anachukua nafsi yake kutoka kwake?[l]
9 Je, Mungu atasikia kilio chake
Taabu ikimjia?[m]
10 Au, je, atapata furaha tele katika Mweza-Yote?

Je, atamwita Mungu
nyakati zote?
11 Nitawafundisha ninyi kwa
mkono wa Mungu;
Mambo yaliyo pamoja na
Mweza-Yote sitayaficha.[a]
12 Tazama! Ninyi nyote
mmeona maono;
Basi kwa nini
mnajionyesha kuwa
wenye ubatili mtupu?[b]
13 Hilo ndilo fungu la mtu
mwovu kutoka kwa
Mungu;[c]
Na urithi wa waonevu
watapokea kutoka kwa
Mweza-Yote mwenyewe.
14 Wanawe wakiwa wengi, ni
kwa ajili ya upanga;[d]
Na wazao wake wenyewe
hawatakuwa na chakula
cha kutosha.
15 Waokokaji wake
mwenyewe watazikwa
wakati wa tauni yenye
kufisha,
Na wajane wao wenyewe
hawatalia.[e]
16 Akirundika fedha kama
mavumbi,
Naye akitayarisha mavazi
kana kwamba ni udongo,
17 Yeye atatayarisha,
lakini mwadilifu ndiye
atakayevaa,[f]
Na yeye asiye na hatia
ndiye atakayekuwa na
fungu katika ile fedha.
18 Ameijenga nyumba yake
kama nondo tu,
Na kama kibanda[g]
ambacho mlinzi
amejenga.
19 Atalala akiwa tajiri,
lakini hakuna chochote
kitakachokusanywa;
Ameyafungua macho yake,
lakini hakutakuwa na
chochote.[h]

SURA 27
a Mdo 20:20
b Yer 23:16
c Zb 11:6
Mhu 8:13
Mal 3:5
d Est 9:10
Ho 9:13
e Zb 78:64
f Met 13:22
Met 28:8
Mhu 2:26
g Isa 1:8
Omb 2:6
h Ayu 14:10

Safu ya 2
a Zb 73:19
b Yer 18:17
c Mt 7:27
d Zb 83:15
Yer 13:14
e Isa 10:3
Amo 2:14
f Hes 24:10
Omb 2:15
Nah 3:19
g 1Fa 9:8
Sef 2:15

SURA 28
h Met 17:3
Mal 3:3
i Kum 8:9
j Mwa 11:6
Lu 1:51
k Amo 9:2
l Mwa 1:11
Zb 104:14
m Ayu 28:16

20 Vitisho vya ghafula
vitampita kama maji;[a]
Upepo wa dhoruba
utamwiba usiku.
21 Upepo wa mashariki
utamchukulia mbali[b]
naye ataenda zake,
Nao utamvurumisha mbali
kutoka mahali pake.[c]
22 Nao utajitupa juu yake
wala hautakuwa na
huruma;[d]
Bila shaka atajaribu
kuzikimbia nguvu zake.[e]
23 Mtu atampigia makofi[f]
Naye atampigia mluzi[g]
kutoka mahali pake.

28 "Kwa kweli, kuna mahali
pa kupata fedha
Na mahali pa dhahabu
ambayo wanasafisha;[h]
2 Chuma hutolewa katika
mavumbi[i]
Na shaba humwagwa
kutoka katika mawe.
3 Ameweka mwisho wa giza;
Naye hutafuta mipaka
yote[j]
Jiwe katika giza na kivuli
kizito.
4 Amechimba shimo mbali
sana na mahali ambapo
watu hukaa ugenini,[k]
Mahali paliposahauliwa,
mbali na mguu;
Baadhi ya wanadamu
wanaoweza kufa
wameshuka chini,
wamening'inia.
5 Kwa habari ya dunia,
chakula hutoka humo;[l]
Lakini chini yake,
imepinduliwa kana
kwamba ni kwa moto.
6 Mawe yake ni mahali pa
yakuti,[m]
Nayo ina vumbi la
dhahabu.

7 Njia—hakuna ndege
mwenye kuwinda[a]
ambaye ameijua,
Wala jicho la mwewe
mweusi[b] halikuiona.
8 Wanyama wa mwituni
wenye fahari
hawajaikanyaga ikawa
ngumu;
Mwana-simba hakutembea
juu yake.
9 Ametia mkono wake juu ya
jiwe gumu;
Ameipindua milima kutoka
katika mizizi yake;
10 Amechimba ndani ya
miamba mifereji iliyojaa
maji,[c]
Na jicho lake limeona vitu
vyote vyenye thamani.
11 Ametengeneza bwawa
mahali ambapo mito
ilitiririka,[d]
Naye hukileta katika nuru
kitu kilichofichwa.
12 Lakini hekima—inaweza
kupatikana wapi,[e]
Na sasa, pako wapi mahali
pa uelewaji?
13 Mwanadamu anayeweza
kufa hajajua thamani
yake,[f]
Nayo haipatikani katika
nchi ya walio hai.
14 Kilindi cha maji kimesema,
'Haimo ndani yangu!'
Bahari pia imesema, 'Haipo
pamoja nami!'[g]
15 Dhahabu safi haiwezi
kubadilishwa nayo,[h]
Wala fedha haiwezi
kupimwa kuwa bei yake.
16 Haiwezi kulipiwa kwa
dhahabu ya Ofiri,[i]
Wala kwa jiwe la
shohamu lisilopatikana
kwa urahisi wala yakuti.

SURA 28

a Eze 39:4

b Law 11:14
Kum 14:13

c 2Fa 20:20
2Nya 32:30

d Isa 44:27
Isa 45:1
Yer 50:38
Yer 51:32

e Ayu 28:28
Met 2:6
Yak 1:5

f Zb 49:7
Met 3:15

g Ro 11:34

h Met 3:14

i Isa 13:12

Safu ya 2

a Met 8:11
Met 20:15

b Met 16:16

c Kut 28:17

d Ayu 28:12
Yak 1:5

e Mhu 8:17
1Ko 2:8

f Met 30:4
Ro 1:20

g Met 15:3
Zek 4:10
1Pe 3:12

h Zb 135:7
Zb 148:8
Mhu 1:6

i Ayu 5:10
Ayu 26:8
Ayu 37:10
Met 30:4
Isa 40:12

j Ayu 38:25
Zek 10:1

17 Dhahabu na kioo haviwezi
kulinganishwa nayo,
Wala chombo chochote cha
dhahabu safi hakiwezi
kubadilishwa nayo.
18 Marijani[a] na fuwele ya
mawe havitatajwa,
Bali mfuko uliojaa hekima
ni wenye thamani kuliko
ule uliojaa lulu.[b]
19 Topazi[c] ya Kushi haiwezi
kulinganishwa nayo;
Haiwezi kulipiwa hata kwa
dhahabu safi.
20 Lakini hekima—hiyo
inatoka wapi,[d]
Na sasa, pako wapi mahali
pa uelewaji?
21 Imefichwa kutoka machoni
pa kila mtu aliye hai,[e]
Nayo imefichwa kutoka
kwa viumbe vinavyoruka
vya mbinguni.
22 Maangamizi na kifo
zimesema,
'Tumesikia habari zake
kwa masikio yetu.'
23 Mungu, Yeye ndiye
ameelewa njia yake,[f]
Naye mwenyewe amejua
mahali pake,
24 Kwa maana yeye
anatazama mpaka
miisho ya dunia;[g]
Anaona chini ya mbingu
zote,
25 Ili kuupima upepo,[h]
Naye ameyapima maji kwa
kipimo;[i]
26 Alipofanyiza sharti kwa
ajili ya mvua,[j]
Na njia kwa ajili ya
wingu la dhoruba lenye
kunguruma,
27 Ndipo alipoiona hekima
kisha akasema habari
zake;

Aliitayarisha na pia
akaichunguza kabisa.
28 Naye akamwambia
mwanadamu,
‘Tazama! Kumwogopa
Yehova—hiyo ndiyo
hekima,[a]
Na kuacha ubaya ni
uelewaji.’”[b]

29 Naye Ayubu akatokeza tena neno lake la kimethali, akaendelea kusema:
2 “Laiti ningekuwa kama
nilivyokuwa katika miezi
ya zamani,[c]
Kama katika siku
ambazo Mungu alikuwa
akinilinda;[d]
3 Wakati alipoangaza taa
yake juu ya kichwa
changu,
Nilipotembea katikati ya
giza kwa nuru yake;[e]
4 Kama nilivyokuwa katika
siku zilizo bora za ujana
wangu,[f]
Wakati urafiki wa karibu
pamoja na Mungu
ulikuwa katika hema
langu;[g]
5 Wakati Mweza-Yote
alipokuwa bado pamoja
nami,
Wakati watumishi wangu
walipokuwa
wamenizunguka pande
zote!
6 Nilipoiosha miguu yangu
katika siagi,
Na mwamba ukaendelea
kunimiminia mito ya
mafuta;[h]
7 Nilipoenda kwenye lango
lililo karibu na mji,[i]
Nilikuwa nikitayarisha kiti
changu katika kiwanja
cha watu wote![j]

SURA 28
a Kum 4:6
Zb 111:10
Met 9:10
Mhu 12:13
Ro 1:20
b Met 3:7
1Pe 3:11

SURA 29
c Ayu 3:6
d Ayu 1:10
e Zb 18:28
Zb 119:105
f Mhu 11:10
g Zb 25:14
Met 3:32
h Kum 32:4
Kum 32:13
Kum 33:24
i Kum 16:18
Ru 4:1
j Ne 8:1

Safu ya 2
a Law 19:32
b Ayu 21:5
c Zb 137:6
d Zb 72:12
Met 21:13
Met 24:11
e Kum 10:18
Yak 1:27
f Kum 24:13
g Kum 10:18
h Kum 24:13
Zb 132:9
Isa 61:10
Efe 6:14
i Hes 10:31
j Lu 14:13
Yak 1:27
k Met 29:7
l Zb 58:6
Met 30:14

8 Wavulana waliniona na
kujificha,
Na hata wazee waliinuka,
walisimama.[a]
9 Wakuu wenyewe walizuia
maneno,
Nao walitia mkono juu ya
vinywa vyao.[b]
10 Sauti ya viongozi ilifichwa,
Na ulimi wao ulishikamana
na kaakaa lao.[c]
11 Kwa maana sikio
lilisikiliza, likanitangaza
kuwa mwenye furaha,
Nalo jicho liliona,
likanishuhudia.
12 Kwa maana nilikuwa
nikimwokoa mwenye
kuteseka anayelia apewe
msaada,[d]
Na mvulana asiye na baba
na mtu yeyote ambaye
hakuwa na msaidizi.[e]
13 Baraka[f] ya mtu aliye
karibu
kuangamia—ilikuwa
ikija juu yangu,
Na moyo wa mjane
nilikuwa nikiufurahisha.[g]
14 Nilivaa uadilifu, nao
ulikuwa ukinivika.[h]
Haki yangu ilikuwa kama
koti lisilo na mikono—na
kilemba.
15 Nilikuwa macho kwa aliye
kipofu;[i]
Nami nilikuwa miguu kwa
aliye kilema.
16 Nilikuwa baba halisi kwa
walio maskini;[j]
Na kesi ya mtu nisiyemjua
nilikuwa nikiichunguza.[k]
17 Nami nilikuwa nikiivunja
mifupa ya taya ya
mkosaji,[l]
Na kutoka katika meno
yake nikawa nikinyakua
mawindo.

18 Na nilikuwa nikisema,
'Nitakata pumzi[a] ndani
ya kiota changu,
Nami nitazidisha siku
zangu kama chembe za
mchanga.[b]
19 Mzizi wangu umefunguliwa
kwa ajili ya maji,[c]
Na umande utakaa usiku
kucha juu ya tawi langu.
20 Utukufu wangu ni mpya
kwangu,
Na upinde wangu mkononi
mwangu utapiga tena na
tena.'
21 Walinisikiliza mimi; nao
wakangojea,
Nao walikuwa wakikaa
kimya wapate shauri
langu.[d]
22 Baada ya neno langu
hawakusema tena,
Na neno langu lilidondoka
juu yao.[e]
23 Nao waliningojea kama
kungojea mvua,[f]
Nao wakakifungua wazi
kinywa chao kwa ajili
ya mvua ya masika.[g]
24 Nilikuwa nikiwapa
tabasamu—wakawa
hawaamini—
Na nuru ya uso[h] wangu
walikuwa hawaizimi.
25 Nilikuwa nikiwachagulia
njia, nami nilikuwa
nikikaa kama kichwa;
Nami nilikaa kama mfalme
katikati ya majeshi yake,[i]
Kama mtu anayewafariji
waombolezaji.[j]

30 "Na sasa wamenicheka,[k]
Wale wenye siku chache
kuliko mimi,[l]
Ambao baba zao
ningekataa
Kuwaweka pamoja na
mbwa wa kundi langu.

SURA 29
a Mwa 25:8
2Fa 22:20
Ayu 42:17
b Zb 30:6
c Zb 1:3
Yer 17:8
d Ayu 29:9
e Eze 21:2
f Zb 72:6
g Met 16:15
h Ayu 30:26
i Ayu 1:3
j Mhu 7:2
1Th 5:11

SURA 30
k Ayu 12:4
l 1Pe 5:5

Safu ya 2
a Isa 1:31
b Yer 17:6
c Mwa 4:12
Zb 109:10
Da 4:25
d 1Sa 25:25
Isa 32:6
e Zb 69:12
Omb 3:14
f Ayu 17:6
g Ayu 19:13
h Hes 12:14
Kum 25:9
Isa 50:6
Mt 27:30

2 Hata nguvu za mikono
yao—zilinifaa nini?
Nguvu zimekwisha ndani
yao.[a]
3 Wao ni tasa kwa sababu ya
upungufu na njaa,
Wanatafuna eneo lisilo na
maji,[b]
Ambapo jana palikuwa na
dhoruba na ukiwa.
4 Walikuwa waking'oa mmea
wa chumvi kando ya
vichaka,
Na mzizi wa miretemu
ulikuwa chakula chao.
5 Walikuwa wakifukuzwa
kutoka katika jamii;[c]
Watu waliwapaazia sauti
kama kupaazia mwizi.
6 Wanalazimika kukaa
kwenye mteremko wa
mabonde ya mito,
Katika matundu ya
mavumbi na katika
miamba.
7 Walilia katikati ya vichaka;
Walisongamana pamoja
chini ya upupu.
8 Wana wa mtu asiye na
akili,[d] pia wana wa mtu
asiye na jina,
Wamepigwa mijeledi
watoke katika nchi.
9 Na sasa mimi nimekuwa
hata kichwa cha wimbo
wao,[e]
Nami ni simango kwao.[f]
10 Wamenichukia, wamekaa
mbali nami;[g]
Nao hawakuacha
kunitemea mate usoni.[h]
11 Kwa kuwa aliifungua
kamba yangu ya upinde
na kuninyenyekeza,
Nao waliifungua lijamu
kwa sababu yangu.
12 Wanasimama upande wa
mkono wangu wa kuume
kama kundi la waovu;

Wameachilia miguu yangu,
Lakini wakajenga juu
yangu vizuizi vyao
vyenye kuleta msiba.[a]
13 Wameziharibu barabara
zangu;
Walizidisha shida kwangu,[b]
Bila wao kuwa na msaidizi
yeyote.
14 Walikuja kana kwamba ni
kupitia pengo pana;
Wamejiviringisha katika
dhoruba.
15 Vitisho vya ghafula
vimegeuzwa juu yangu;
Cheo changu cha heshima
kinafukuzwa kama
upepo,
Na wokovu wangu
umepitilia mbali kama
wingu.
16 Na sasa nafsi
yangu inamwagwa ndani
yangu;[c]
Siku za mateso[d]
zinanishika.
17 Mifupa[e] yangu
imetobolewa usiku na
kuanguka kutoka
kwangu,
Na
maumivu
yanayonitafuna
hayapumziki.[f]
18 Vazi langu linabadilika
kutokana na wingi wa
nguvu;
Linanifunga kama ukosi
wa vazi langu refu.
19 Amenishusha chini katika
udongo,
Hivi kwamba nimekuwa
kama mavumbi na
majivu.
20 Ninakulilia nipate msaada,
lakini wewe hunijibu;[g]
Nimesimama, ili unikazie
fikira.

SURA 30
a Ayu 19:12
b Ayu 16:2
Zb 69:26
c Zb 22:14
d Ayu 10:15
e Zb 6:2
f Ayu 2:8
Ayu 2:13
Ayu 7:4
g Ayu 19:7
Zb 22:2
Omb 3:8

Safu ya 2
a Ayu 7:20
Ayu 19:6
b Mwa 3:19
c Ayu 13:25
d Zb 35:13
Ro 12:15
e Met 14:21
Met 14:31
Met 19:17
f Yer 8:15
Yer 14:19
g Zb 38:6
Zb 42:9
Zb 43:2
h Mik 1:8

21 Unajibadili ili uwe mkatili
kwangu;[a]
Unadumisha uadui kwangu
kwa nguvu kamili za
mkono wako.
22 Unaniinua kwenye upepo,
unanifanya niupande;
Kisha unaniyeyusha kwa
kishindo.
23 Kwa maana najua vema
kwamba utanirudisha
kwenye kifo,[b]
Na kwenye nyumba ya
kukutania ya kila mtu
aliye hai.
24 Ila tu hakuna yeyote
anayeunyoosha mkono
wake juu ya rundo la
mabomoko matupu,[c]
Wala wakati wa kudhoofika
kwa mtu hakuna kilio
cha kuomba msaada
kuhusu mambo hayo.
25 Hakika nimemlilia mtu
aliye na siku ngumu;[d]
Nafsi yangu
imemhuzunikia maskini.[e]
26 Ijapokuwa nilingojea
mema, mabaya yalikuja;[f]
Nami nikaendelea
kungojea nuru, lakini
giza likaja.
27 Matumbo yangu
yalichemshwa wala
hayakukaa kimya;
Siku za mateso zilinikabili.
28 Nilitembea huku na huku
kwa huzuni[g] wakati
ambapo hakukuwa nuru
ya jua;
Nilisimama katika
kutaniko, nikaendelea
kulia nipewe msaada.
29 Nikawa ndugu ya
mbwa-mwitu,
Na rafiki ya binti za
mbuni.[h]

30 Ngozi yangu ikawa nyeusi[a]
na kuanguka kutoka
kwangu,
Na mifupa yangu ikawaka
moto kutokana na
ukavu.
31 Na kinubi changu kikawa
cha maombolezo matupu,
Na zumari yangu kwa
ajili ya sauti ya watu
wanaolia.

31 "Nimefanya agano
pamoja na macho
yangu.[b]
Basi nawezaje kukaza
fikira kwa bikira?[c]
2 Na kuna fungu gani
kutoka kwa Mungu juu,[d]
Au urithi kutoka kwa
Mweza-Yote kutoka juu?
3 Je, hakuna msiba kwa
mkosaji,[e]
Na maafa kwa
wale wanaozoea kufanya
madhara?
4 Je, yeye haoni njia zangu[f]
Na kuzihesabu hata hatua
zangu zote?
5 Ikiwa nimetembea na watu
wasiosema kweli,[g]
Na mguu wangu
unaharakisha kuelekea
udanganyifu,[h]
6 Atanipima katika mizani
sahihi[i]
Na Mungu atajua utimilifu
wangu.[j]
7 Ikiwa hatua zangu
zinageuka kutoka katika
njia,[k]
Au moyo wangu
umetembea kwa kufuata
macho yangu tu,[l]
Au kasoro yoyote
imeshikamana na
mikono yangu,[m]
8 Acha nipande mbegu na
kisha mwingine ale,[n]
Na acha wazao wangu
wang'olewe.
9 Ikiwa moyo wangu
umeshawishiwa
kumwelekea
mwanamke,[a]
Nami nikaendelea kuvizia[b]
katika mlango wa rafiki
yangu,
10 Basi mke wangu na
amsagie mwanamume
mwingine,
Wanaume wengine na
wainame juu yake.[c]
11 Kwa maana jambo hilo
lingekuwa mwenendo
mpotovu,
Nalo lingekuwa kosa la
kufikiriwa na waamuzi.[d]
12 Kwa maana huo ni moto
ambao ungeteketeza
mpaka kwenye
maangamizi,[e]
Na katikati ya mazao
yangu yote ungetia
mizizi.
13 Ikiwa nilikuwa nikikataa
hukumu ya haki ya
mtumwa wangu
Au ya kijakazi wangu
katika kesi yao juu
yangu,
14 Basi naweza kufanya
nini wakati Mungu
atakaposimama?
Na wakati atakapotoza
hesabu, naweza kumjibu
nini?[f]
15 Je, Yeye aliyenifanya mimi
tumboni hakumfanya
yeye,[g]
Na je, si yeye Mmoja tu
aliyetufanya sisi katika
tumbo la uzazi?
16 Ikiwa nilikuwa
nikiwanyima watu wa
hali ya chini mapendezi
yao,[h]

SURA 30
a Ayu 7:5
Zb 119:83
Omb 4:8

SURA 31
b Met 6:25
Mt 5:28
c Ayu 31:9
1Ko 7:1
d Ayu 20:29
e Zb 73:18
Met 10:29
f Mwa 16:13
2Nya 16:9
Zb 139:3
Met 5:21
Yer 32:19
g Zb 26:5
h Met 6:18
i 1Sa 2:3
Da 5:27
j Ayu 2:3
Ayu 27:5
Zb 7:8
k Kum 11:16
Yer 10:23
l Hes 15:39
Mhu 11:9
Eze 6:9
Mt 5:29
1Yo 2:16
m Isa 33:15
n Law 26:16

Safu ya 2
a Ayu 31:1
Mt 5:28
b Ayu 24:15
c 2Sa 12:11
Yer 8:10
d Mwa 38:24
Law 20:10
Kum 22:22
e Met 6:27
Met 7:27
f Zb 82:3
Met 22:23
Isa 10:3
g Ayu 34:19
Zb 139:16
Met 14:31
Met 22:2
Mal 2:10
h Kum 15:7

Na kuyafanya macho ya
mjane yaishiwe nguvu,[a]
17 Na kula tonge langu peke
yangu,
Huku mvulana asiye
na baba akiwa hali
kutokana nalo[b]
18 (Kwa maana tangu ujana
wangu alikua pamoja
nami kana kwamba
pamoja na baba,
Na kutoka tumboni mwa
mama yangu niliendelea
kumwongoza huyo
mjane);
19 Ikiwa nilikuwa nikiona
mtu yeyote akiangamia
kwa kukosa vazi,[c]
Au kwamba maskini
hakuwa na cha
kujifunika;
20 Ikiwa viuno vyake
havikunibariki,[d]
Wala hakujipasha moto
kwa sufu[e] iliyokatwa ya
wana-kondoo wangu;
21 Ikiwa nilitikisa mkono
wangu huku na huku juu
ya mvulana asiye na
baba,[f]
Wakati nilipokuwa
nikiona msaada wangu
unahitajiwa katika
lango,[g]
22 Acha mfupa wa bega langu
uanguke kutoka katika
bega lake,
Na acha mkono wangu
uvunjwe kutoka kwenye
mfupa wake wa juu.
23 Kwa maana msiba kutoka
kwa Mungu ulinitia hofu,
Nami sikuweza kuvumilia
mbele ya utukufu[h] wake.
24 Ikiwa nimeifanya dhahabu
kuwa tumaini langu,
Au nimeiambia dhahabu,
‘Wewe ni tegemeo langu!’[i]

SURA 31
a Kum 10:18
Met 28:27
b Eze 18:7
Yak 1:27
1Yo 3:17
c Isa 58:7
Mt 25:36
Lu 3:11
Yak 2:15
d Kum 24:13
e Kum 18:4
f Met 14:21
g Kum 16:18
h Ayu 13:11
i Zb 49:6
Met 11:28
1Ti 6:17

Safu ya 2
a Est 5:11
Zb 62:10
Met 11:28
b Kum 8:17
c Kum 4:19
d Kum 11:16
e Met 17:5
Met 24:17
f Mt 5:44
Ro 12:14
g Mwa 18:5
Ro 12:13
h Mwa 19:3
Amu 19:21
Mt 25:35
Ebr 13:2
1Pe 4:9
i Mwa 3:8
Met 28:13
Mdo 5:8

25 Ikiwa nilikuwa
nikishangilia kwa sababu
mali yangu ilikuwa
nyingi,[a]
Na kwa sababu mkono
wangu ulikuwa umepata
vitu vingi sana;[b]
26 Ikiwa nilikuwa nikiona
nuru wakati ilipowaka,
Au mwezi wenye fahari
ukisonga,[c]
27 Na moyo wangu ukaanza
kushawishiwa kisiri[d]
Na mkono wangu
ukakibusu kinywa
changu,
28 Hilo pia lingekuwa kosa la
kufikiriwa na waamuzi,
Kwa maana ningekuwa
nimemkana Mungu wa
kweli aliye juu.
29 Ikiwa nilikuwa
nikishangilia kuangamia
kwa mtu anayenichukia
vikali,[e]
Au kuchangamka
kwa sababu uovu
umempata—
30 Nami sikuruhusu kaakaa
langu kutenda dhambi
Kwa kuomba laana juu ya
nafsi yake.[f]
31 Ikiwa watu wa hema langu
hawakusema,
‘Ni nani anayeweza
kutokeza mtu ambaye
hakushibishwa na
chakula chake?’[g]—
32 Hakuna mkaaji mgeni
yeyote aliyelala nje
usiku;[h]
Milango yangu niliiacha
wazi kuielekea njia.
33 Ikiwa kama mtu wa udongo
niliyafunika makosa
yangu[i]
Kwa kuficha kosa langu
katika mfuko wa shati
langu—

34 Kwa kuwa nilikuwa
nikishtuka kwa sababu
ya umati mkubwa,
Au dharau la familia
lilikuwa likinitia hofu
Nami nilikuwa nikikaa
kimya, sikuwa
nikiondoka nje ya
mlango.
35 Laiti ningekuwa na mtu
wa kunisikiliza,[a]
Kwamba Mweza-Yote
angenijibu[b] kulingana na
sahihi yangu!
Au kwamba mtu aliye
na kesi juu yangu
angeandika hati!
36 Hakika ningeibeba juu ya
bega langu;
Ningeifunga kunizunguka
kama taji la fahari.
37 Ningemwambia hesabu ya
hatua zangu;[c]
Ningemwendea kama
kiongozi.
38 Ikiwa nchi yangu ingelia
kwa sababu yangu ipate
msaada,
Na mitaro yake ingelia
pamoja;
39 Ikiwa nimekula matunda
yake bila pesa,[d]
Na nafsi ya wamiliki wake
nimeifanya ipumue,[e]
40 Basi magugu yenye miiba
na yatokee badala ya
ngano,[f]
Na magugu yenye kunuka
badala ya shayiri."

Maneno ya Ayubu yamefika mwisho.

32 Basi hao watu watatu wakaacha kumjibu Ayubu, kwa sababu alikuwa mwadilifu machoni pake mwenyewe.[g] **2** Lakini hasira ya Elihu mwana wa Barakeli, Mbuzi,[h] wa familia ya Ramu, ikawaka. Hasira yake ikamwakia Ayubu kwa sababu aliitangaza nafsi yake mwenyewe kuwa adilifu badala ya Mungu.[a] **3** Pia, hasira yake ikawaka juu ya wale rafiki zake watatu kwa sababu hawakupata jibu bali walimtangaza Mungu kuwa mwovu.[b] **4** Naye Elihu alikuwa amemngojea Ayubu kwa maneno, kwa sababu walikuwa wazee kwa siku kuliko yeye.[c] **5** Na mwishowe Elihu akaona kwamba hakuna jibu kinywani[d] mwa wale watu watatu, na hasira yake ikazidi kuwaka. **6** Ndipo Elihu mwana wa Barakeli, Mbuzi, akajibu, akasema:

"Mimi ni kijana katika siku
Nanyi ni wazee.[e]
Ndiyo sababu nilikaa mbali
nikaogopa
Kuwatangazia ninyi ujuzi
wangu.
7 Nilisema, 'Siku zinapaswa
kusema,
Na wingi wa miaka ndio
unaopaswa kujulisha
hekima.'[f]
8 Hakika ni roho iliyo
ndani ya wanadamu
wanaoweza kufa
Na pumzi ya Mweza-Yote
ndiyo inayowapa wao
uelewaji.[g]
9 Si wale walio na siku
nyingi tu ndio huwa na
hekima,[h]
Wala si wale walio wazee tu
ndio huelewa hukumu.[i]
10 Kwa hiyo nikasema,
'Nisikilize mimi.
Nami, naam, mimi
nitautangaza ujuzi
wangu.'
11 Tazama! Nimeyangojea
maneno yenu,

SURA 31
a Ayu 19:7
b Ayu 13:22
c Ayu 29:6
d Yak 5:4
e 1Fa 21:15
f Mwa 3:18

SURA 32
g Ayu 6:29
Ayu 27:6
Met 3:7
h Mwa 22:21

Safu ya 2
a Ayu 10:3
b Kut 20:7
Ayu 4:18
Ayu 22:3
Ayu 25:5
Ayu 42:8
c Law 19:32
d Zb 78:36
2Ko 13:1
Tit 1:11
e Ayu 15:10
1Ti 5:1
1Pe 5:5
f 1Fa 12:6
Ayu 12:12
g 1Fa 3:12
1Fa 4:29
Ayu 35:11
Met 2:6
Mhu 2:26
Da 1:17
Mt 11:25
Yak 1:5
h Zb 119:100
1Ko 1:26
i Mhu 4:13

Niliendelea kutega sikio
kwa namna yenu ya
kufikiri,[a]
Mpaka mweze kutafuta
maneno ya kusema.
12 Nami nikaendelea
kuwakazia ninyi fikira,
Na tazama, hakuna yeyote
anayemkaripia Ayubu,
Hakuna yeyote kati yenu
anayejibu maneno yake,
13 Kwa hiyo msiseme,
'Tumepata hekima;[b]
Ni Mungu anayemfukuzia
mbali, wala si
mwanadamu.'
14 Kwa kuwa hajapanga
maneno juu yangu,
Kwa hiyo sitamjibu yeye
kwa maneno yenu.
15 Wametishika, hawakujibu
tena;
Maneno yamewaondoka.
16 Nami nimengojea, kwa
maana hawaendelei
kusema;
Kwa maana walisimama
tuli, hawakujibu tena.
17 Nami, naam, mimi nitajibu
sehemu yangu;
Nami, naam, mimi
nitautangaza ujuzi
wangu;
18 Kwa maana nimejaa
maneno;
Roho imeleta mkazo[c] juu
yangu ndani ya tumbo
langu.
19 Tazama! Tumbo langu ni
kama divai iliyozibwa;
Linataka kupasuka kama
viriba vipya.[d]
20 Acha niseme ili nipate
kitulizo.
Nitaifungua midomo yangu
nipate kujibu.[e]
21 Tafadhali, acha
nisionyeshe upendeleo
kwa mwanadamu;[f]

SURA 32
a Yak 1:19
b Yer 9:23
1Ko 1:29
c Zb 39:3
Yer 20:9
Mdo 18:25
d Mt 9:17
e Met 15:28
1Pe 3:15
f Law 19:15
Met 24:23
Yak 3:17

Safu ya 2
a Mt 23:8
Lu 18:19
b Ayu 27:8
Ayu 35:10
Zb 95:6

SURA 33
c Ayu 6:30
Zb 137:6
d Mt 12:34
Lu 6:45
e Met 15:2
Met 20:15
f Zb 119:73
g Mwa 2:7
Ayu 32:8
Mhu 12:7
Mdo 17:25
h Mdo 14:15
i Mwa 2:7
Ayu 10:9
1Ko 15:47
2Ko 4:7
j Amu 16:16
Lu 24:29

Nami sitampa mtu wa
udongo jina la cheo;[a]
22 Kwa maana hakika sijui
jinsi ninavyoweza kutoa
jina la cheo;
Mtengenezaji[b] wangu
angenichukulia mbali
kwa urahisi.

33 "Hata hivyo, sasa, Ee
Ayubu, tafadhali sikia
maneno yangu,
Nawe tega sikio kwa
maneno yangu yote.
2 Tafadhali, tazama! Lazima
nifungue kinywa
changu;
Ulimi wangu pamoja na
kaakaa[c] langu lazima
viseme.
3 Maneno yangu ni unyoofu
wa moyo wangu,[d]
Na midomo yangu hutamka
ujuzi kwa unyoofu.[e]
4 Roho ya Mungu ilinifanya
mimi,[f]
Na pumzi ya Mweza-Yote
mwenyewe ikanifanya
kuwa hai.[g]
5 Ukiweza, nijibu,
Yapange maneno mbele
yangu; usimame mahali
pako.
6 Tazama! Mimi ni kama
wewe tu[h] mbele za
Mungu wa kweli;
Mimi pia niliumbwa kutoka
kwenye udongo.[i]
7 Tazama! Hofu yoyote
kutoka kwangu
haitakutisha,
Wala mkazo[j] kutoka
kwangu hautakuwa
mzito juu yako.
8 Ila tu umesema masikioni
mwangu,
Nami nikaendelea kusikia
sauti ya maneno yako,

9 ‘Mimi ni safi bila makosa;[a]
Mimi ni safi, wala sina
kosa.[b]
10 Tazama! Anatafuta sababu
za kunipinga,
Ananichukua mimi kuwa
adui yake.[c]
11 Anaiweka miguu yangu
katika mikatale,[d]
Anaziangalia njia zangu
zote.’[e]
12 Tazama! Katika hayo
hukuwa upande wa haki,[f]
ninakujibu;
Kwa maana Mungu
anamzidi mwanadamu
anayeweza kufa.[g]
13 Kwa nini ulishindana
naye,[h]
Kwa sababu hajibu maneno
yako yote?[i]
14 Kwa maana Mungu
husema mara moja,
Na mara mbili[j]—ingawa
mtu hafikirii hayo—
15 Katika ndoto,[k] maono[l] ya
usiku,
Wakati usingizi mzito
unapowashika
wanadamu,
Wakati wa kusinzia
kitandani.[m]
16 Ndipo anapofungua sikio la
wanadamu,[n]
Naye hutia muhuri wake
kwa kuwasihi wao,
17 Ili kumgeuza mwanadamu
kutoka katika tendo
lake,[o]
Na ili afunike
kiburi[p] kutoka kwa
mwanamume.
18 Anazuia nafsi yake isiingie
katika shimo[q]
Na uzima wake usipitilie
mbali kwa silaha.[r]
19 Naye kwa kweli
hukaripiwa kwa
maumivu kitandani
mwake,
Na kugombana kwa
mifupa yake huendelea
mfululizo.
20 Na uzima wake kwa
hakika hufanya mkate
uchukize,[a]
Na nafsi yake chakula
kinachotamaniwa.
21 Nyama yake hukonda
ikaacha kuonekana,
Na mifupa yake ambayo
haikuonekana hakika
hutokeza.
22 Na nafsi yake hukaribia
kwenye shimo,[b]
Na uzima wake kwa wale
wanaosababisha kifo.
23 Ikiwa kuna mjumbe kwa
ajili yake,
Msemaji, mmoja kati ya
elfu,
Ili kumwambia
mwanadamu unyoofu
wake,
24 Ndipo anapompa kibali na
kusema,
‘Mwachilie ili asishuke
chini kuingia shimoni![c]
Nimepata fidia![d]
25 Nyama yake na iwe laini
kuliko wakati wa ujana;[e]
Na arudi kwenye siku za
nguvu za ujana wake.’[f]
26 Yeye atamsihi Mungu ili
amfurahie,
Naye ataona uso wake
kwa kupaaza sauti kwa
shangwe,[g]
Na Yeye ataurudisha
uadilifu Wake kwa
mwanadamu anayeweza
kufa.
27 Yeye atawaimbia
wanadamu na kusema,
‘Nimetenda dhambi;[h] na
nimepotosha lililo
nyoofu,

SURA 33

a Ayu 10:7
Ayu 16:17
Ayu 23:11
b Ayu 29:14
Met 21:2
c Ayu 13:24
Ayu 16:9
Ayu 19:11
d Ayu 13:27
Yer 20:2
Mdo 16:24
e Ayu 14:16
Ayu 31:4
f Met 9:8
Ga 2:11
g Ayu 12:13
Zb 8:4
Isa 40:25
Isa 55:9
h Isa 45:9
Ro 9:20
1Ko 10:22
i Ayu 13:24
j Ayu 40:5
Zb 62:11
k Da 4:5
l Hes 12:6
m Da 4:5
n Ayu 36:10
o Mwa 20:6
Mt 2:12
Mt 27:19
p Da 4:25
q Mwa 31:24
r 2Nya 32:5
Efe 6:16

Safu ya 2

a Zb 107:18
b Zb 89:48
c Ayu 14:13
d Ayu 19:25
Zb 49:7
Mt 20:28
e 2Fa 5:14
f Kum 34:7
Ayu 42:16
Zb 103:5
g Zb 30:8
h 2Sa 12:13
Zb 32:5
Met 28:13
Lu 15:21
1Yo 1:9

Nalo hakika halikuwa
jambo linalofaa kwangu.
28 Yeye ameikomboa nafsi
yangu isiingie shimoni,[a]
Na uzima wangu wenyewe
utaona nuru.'
29 Tazama! Mungu hufanya
mambo hayo yote,
Mara mbili, mara
tatu, kuhusiana na
mwanamume,
30 Ili kuigeuza nafsi yake
isiingie shimoni,[b]
Ili atiwe nuru kwa nuru ya
wale walio hai.[c]
31 Kaza uangalifu, Ee Ayubu!
Nisikilize mimi!
Nyamaza kimya, nami
nitaendelea kusema.
32 Ikiwa kuna maneno yoyote
ya kusema, nijibu;
Sema, kwa maana
nimependezwa na
uadilifu wako.
33 Ikiwa hakuna yoyote,
basi wewe mwenyewe
nisikilize mimi;[d]
Nyamaza kimya, nami
nitakufundisha hekima."

34 Naye Elihu akaendelea
kujibu, akasema:
2 "Sikilizeni maneno yangu,
enyi wenye hekima;
Nanyi mnaojua, nitegeeni
sikio.
3 Kwa maana sikio hupima
maneno,[e]
Kama vile kaakaa
linavyoonja wakati wa
kula.[f]
4 Acheni tujichagulie
hukumu;
Acheni tujue yaliyo mema
katikati yetu.
5 Kwa maana Ayubu
amesema, 'Hakika mimi
niko upande wa haki,[g]

SURA 33
a Zb 19:14
Isa 38:17
b Ayu 33:24
c Zb 56:13
d Zb 34:11

SURA 34
e Ayu 12:11
Mdo 17:11
Ufu 2:7
f Ayu 6:30
g Ayu 29:14
Ayu 33:9

Safu ya 2
a Ayu 27:2
b Ayu 9:17
c Ayu 2:3
Eze 14:20
Yak 5:11
d Ayu 15:16
Mt 5:39
e Met 1:15
Met 4:14
f Ayu 9:22
Ayu 35:3
Mal 3:14
g Ayu 34:34
h Mwa 18:25
2Nya 19:7
Zb 92:15
i Kum 32:4
Ro 9:14
Ebr 6:10
j 1Nya 28:9
Zb 62:12
Met 24:12
Yer 32:19
Eze 33:20
Mt 16:27
Ro 2:6
2Ko 5:10
Ga 6:7
1Pe 1:17
Ufu 22:12
k Ayu 8:3
Yak 1:13
l Zb 89:14
Zb 97:2
Zb 99:4
Ro 2:11
m Ayu 27:3
Zb 104:29
Mhu 12:7
Isa 42:5
Mdo 17:25

Lakini Mungu ameigeuza
hukumu yangu.[a]
6 Je, mimi nasema uwongo
juu ya hukumu yangu
mwenyewe?
Jeraha langu kali haliponi
ingawa hakuna kosa.'[b]
7 Ni mwanamume gani aliye
kama Ayubu,[c]
Ambaye hunywa dharau
kama maji?[d]
8 Naye hakika ameenda
kushirikiana na
wanaotenda madhara
Na kwenda kutembea
pamoja na watu waovu.[e]
9 Kwa maana yeye amesema,
'Mwanadamu hapati
faida[f]
Kwa kumfurahia Mungu.'
10 Kwa hiyo nisikilizeni mimi,
ninyi watu walio na moyo
wenye kufahamu.[g]
Hasha, Mungu wa kweli
asitende kwa uovu,[h]
Na Mweza-Yote kutenda
isivyo haki![i]
11 Kwa maana yeye atamlipa[j]
mtu wa udongo
kulingana na matendo
yake,
Na kulingana na pito la
mwanadamu yeye
ataifanya ije juu yake.
12 Ndiyo, kwa kweli, Mungu
hatendi kwa uovu,[k]
Na Mweza-Yote hapotoshi
hukumu.[l]
13 Ni nani aliyemgawia dunia,
Na ni nani aliyemwekea
nchi yenye kuzaa, hiyo
yote?
14 Akikaza moyo wake juu ya
mtu yeyote,
Akijikusanyia kwake roho
na pumzi ya mtu huyo,[m]
15 Mwili wote utakata pumzi
pamoja,

Na mtu wa udongo atarudi
kwenye mavumbi.[a]
16 Basi ikiwa una uelewaji,
sikiliza mambo haya;
Tega sikio kwa sauti ya
maneno yangu.
17 Kwa kweli, je, mtu
yeyote anayechukia haki
ataongoza,[b]
Na ikiwa mwenye nguvu
ni mwadilifu, je,
utamtangaza yeye kuwa
mwovu?[c]
18 Je, mtu atamwambia
mfalme, 'Wewe hufai
kitu'?
Atawaambia watu wenye
vyeo, 'Ninyi ni waovu'?[d]
19 Yupo Yeye ambaye
hajaonyesha upendeleo
kwa wakuu
Wala hakumwonyesha
mwenye cheo ufikirio
kuliko yule wa hali ya
chini,[e]
Kwa maana wao wote ni
kazi ya mikono yake.[f]
20 Wanakufa ghafula,[g]
katikati ya usiku;[h]
Watu huyumba-yumba na
kupitilia mbali,
Na wenye nguvu
huondolewa pasipo
mkono wa mtu.[i]
21 Kwa maana macho yake
yako juu ya njia za
mwanadamu,[j]
Naye huziona hatua zake
zote.
22 Hakuna giza wala kivuli
kizito
Kwa ajili ya wale
wanaozoea kufanya
madhara kujificha humo.[k]
23 Kwa maana haweki wakati
wowote kwa ajili ya
mwanadamu yeyote
Aende kwa Mungu
hukumuni.

SURA 34

a Mwa 3:19
Zb 146:4
Mhu 3:20
b 2Sa 23:3
c Mwa 18:25
d Kut 22:28
Met 17:26
Mhu 8:4
Mhu 10:20
e Kum 10:17
2Nya 19:7
Mdo 10:34
Ro 2:11
Ga 2:6
Efe 6:9
f Ayu 31:15
Met 22:2
g Zb 73:19
Mdo 12:23
h Kut 12:29
Da 5:30
Lu 12:20
i 1Sa 25:38
Da 2:34
j Mwa 6:5
2Nya 16:9
Ayu 31:4
Met 5:21
Met 15:3
Yer 16:17
Yer 32:19
1Pe 3:12
k Zb 139:12
Isa 29:15
Yer 23:24
Amo 9:3
Ebr 4:13

Safu ya 2

a Da 2:21
b Eze 21:27
Da 4:25
c Ho 7:2
2Ko 11:15
Tit 1:16
d 1Sa 4:17
Da 5:30
e Hes 12:10
f Kut 32:8
1Sa 15:11
g Zb 28:5
Isa 5:12
h Kut 22:23
Ayu 35:9
Yak 5:4
i Zb 27:9
Zb 30:7
j Ho 4:6
k Ayu 13:16
Ayu 27:8
l 1Fa 12:28
2Fa 21:9
m Da 9:7
Ro 3:23
n Met 28:13

24 Yeye huwavunja wenye
nguvu[a] bila uchunguzi
wowote,
Naye husimamisha
wengine badala yao.[b]
25 Kwa hiyo yeye hutambua
kazi zao zilivyo,[c]
Naye huwapindua usiku,
nao hupondwa.[d]
26 Yeye huwapiga kofi kwa
kuwa ni waovu
Mahali pa watazamaji;[e]
27 Kwa sababu wamegeuka
kando wasimfuate,[f]
Nao hawakufikiria yoyote
ya njia zake,[g]
28 Ili kukifanya kilio cha mtu
wa hali ya chini kimfikie;
Na hivyo yeye hukisikia
kilio cha watu
wanaoteseka.[h]
29 Yeye mwenyewe
anaposababisha utulivu,
ni nani, basi, anayeweza
kulaumu?
Na anapoficha uso wake,[i]
ni nani anayeweza
kumwona,
Iwe ni kuelekea taifa[j] au
ni kuelekea mwanadamu,
yote yakiwa ni mamoja?
30 Ili mwasi-imani asitawale,[k]
Wala pasiwe na mitego[l] ya
watu.
31 Kwa maana, je, yeyote
atamwambia Mungu
mwenyewe,
'Mimi nimevumilia,
ijapokuwa sitendi kwa
ufisadi;[m]
32 Ijapokuwa sioni lolote,
nifundishe wewe
mwenyewe;
Ikiwa nimetenda ukosefu
wowote wa uadilifu,
Sitautenda tena'?[n]
33 Je, yeye atalilipia
kama unavyopenda kwa

sababu unakataa
hukumu,
Kwa sababu wewe
mwenyewe unachagua,
wala si mimi?
Unalolijua vema, liseme.
34 Watu wenye moyo wa
kuelewa[a] wataniambia—
Hata mwanamume
mwenye hekima
anayenisikiliza,
35 'Ayubu mwenyewe
anasema bila ujuzi,[b]
Na katika maneno yake
hana ufahamu.'
36 Baba yangu, Ayubu na
ajaribiwe mpaka ukomo
Juu ya majibu yake katikati
ya watu wenye madhara.[c]
37 Kwa maana anaongeza
maasi juu ya dhambi
yake;[d]
Anapiga makofi katikati
yetu na kuzidisha
maneno yake dhidi ya
Mungu wa kweli!"[e]

35 Naye Elihu akaendelea
kujibu, akasema:
2 "Je, haya ndiyo umeyaona
kuwa haki?
Wewe umesema, 'Uadilifu
wangu unazidi wa
Mungu.'[f]
3 Kwa maana unasema, 'Ni
wa faida gani kwako?[g]
Ninapata faida gani
zaidi kuliko nikitenda
dhambi?'[h]
4 Mimi nitakujibu wewe
Na rafiki zako[i] pamoja
nawe.
5 Tazama juu mbinguni[j]
uone,
Na yaangalie mawingu,[k]
kwamba kwelikweli yako
juu kuliko wewe.
6 Kwa kweli ukitenda
dhambi, ni nini
unachotimiza dhidi
yake?[a]
Na maasi yako kwa kweli
yakiongezeka,
unamtendea nini?
7 Ikiwa kweli uko upande wa
haki, unampa nini,
Au, je, yeye anapokea
nini kutoka mkononi
mwako?[b]
8 Uovu wako unaweza kuwa
juu ya mwanadamu
kama wewe,[c]
Na uadilifu wako kwa
mwana wa mtu wa
udongo.[d]
9 Kwa sababu ya
ukandamizaji mwingi
wanaendelea kuomba
msaada;[e]
Wanaendelea kulia wapewe
msaada kwa sababu ya
mkono wa wakuu.[f]
10 Na ingawa hivyo hakuna
yeyote ambaye amesema,
'Yuko wapi Mungu,
Mtengenezaji Mkuu
wangu,[g]
Yeye anayetoa muziki
wakati wa usiku?'[h]
11 Ni Yeye anayetufundisha[i]
sisi kuliko wanyama wa
dunia,[j]
Naye anatufanya tuwe
na hekima kuliko hata
viumbe vinavyoruka vya
mbinguni.
12 Huko wao huendelea
kupaaza kilio, lakini
yeye hajibu,[k]
Kwa sababu ya kiburi[l] cha
wabaya.
13 Yasiyo ya kweli tu ndiyo
Mungu hasikii,[m]
Na Mweza-Yote mwenyewe
hayatazami.[n]
14 Sembuse basi unaposema
kwamba humwoni![o]

SURA 34
a Ayu 34:10
b Ayu 35:16
Ayu 38:2
Ayu 42:3
c Yak 5:11
1Pe 1:7
d Ayu 10:1
Ayu 19:6
e Ayu 35:2

SURA 35
f Ayu 10:7
Ayu 16:17
Ayu 34:5
g Ayu 21:15
Ayu 34:9
h Ayu 9:22
Zb 73:13
Mal 3:14
i Ayu 2:11
j Ayu 22:12
k Zb 68:34

Safu ya 2
a Met 8:36
Met 9:12
Yer 7:19
b Zb 16:2
Ro 11:35
c Met 19:3
Ga 6:7
d Eze 33:16
e Kut 2:23
Ayu 34:28
Met 29:2
f Zb 10:15
g Isa 51:13
1Pe 4:19
Ufu 4:11
h Zb 42:8
Zb 77:6
Zb 149:5
Mdo 16:25
i Zb 94:12
Isa 48:17
j Mwa 1:26
Met 30:24
k Zb 18:41
Met 1:28
l 1Pe 5:5
m Met 15:29
Isa 1:15
Yer 11:11
n Hab 1:13
o Ayu 9:11

Kesi iko mbele zake,
na kwa hiyo unapaswa
umngojee kwa hangaiko.[a]
15 Na sasa kwa sababu hasira
yake haijatoza hesabu,[b]
Yeye pia hakufuatilia kule
kuchukua hatua kwa
haraka inayopita kiasi.[c]
16 Na Ayubu mwenyewe
hukifungua wazi kinywa
chake bure tu;
Anazidisha maneno
matupu pasipo ujuzi.”[d]

36 Naye Elihu akaendelea
kusema:
2 “Nisubiri kidogo, nami
nitakutangazia
Kwamba bado kuna
maneno ya kusema kwa
ajili ya Mungu.
3 Nitachukua ujuzi wangu
kutoka mbali,
Nami nitamhesabia
uadilifu Muumba wangu.[e]
4 Kwa maana maneno yangu
kwa kweli si uwongo;
Yeye aliye mkamilifu
katika ujuzi[f] yuko
pamoja nawe.
5 Tazama! Mungu ni mwenye
nguvu[g] wala hatakataa;
Yeye ana uwezo wa nguvu
za moyo;
6 Hatamhifadhi hai mtu
yeyote aliye mwovu,[h]
Lakini atatoa hukumu ya
wenye kuteseka.[i]
7 Hataondoa macho yake juu
ya mtu yeyote aliye
mwadilifu;[j]
Hata wafalme juu ya kiti
cha ufalme[k]—
Yeye pia atawaketisha
milele, nao watainuliwa.
8 Na ikiwa wamefungwa
pingu,[l]
Wanatekwa kwa kamba za
mateso.

SURA 35
a Zb 37:5
b Zb 89:32
c Zb 103:12
d Ayu 34:35
Ayu 38:2

SURA 36
e Kum 32:4
Zb 11:7
Zb 139:14
Zb 139:16
Da 9:14
Ufu 15:3
f 1Sa 2:3
Ayu 37:16
g Zb 24:8
Zb 99:4
Yer 32:18
h Zb 9:17
Zb 68:2
2Pe 2:9
i Zb 10:14
Zb 140:12
Met 22:23
j Zb 33:18
Zb 34:15
k Zb 78:70
Zb 113:8
Isa 9:7
l Zb 107:10

Safu ya 2
a Zb 33:16
b Eze 18:30
c Isa 1:19
Yer 26:13
d Isa 1:20
Ro 2:8
e Ayu 33:18
f Ayu 13:16
Ro 2:5
g Zb 55:23
h 1Fa 14:24
i Isa 30:21
j Zb 18:19
Zb 31:8
Zb 118:5
k Isa 25:6
Isa 55:2
l Met 2:22
Yer 25:31

9 Ndipo atawaambia kuhusu
jinsi wanavyotenda
Na makosa yao, kwa
sababu wanajivuna sana.
10 Naye atafungua sikio lao ili
lisikie himizo,[a]
Naye atasema kwamba
wageuke waache
madhara.[b]
11 Wakitii na kutumikia,
Watakamilisha siku zao
katika mema
Na miaka yao katika uzuri.[c]
12 Lakini wasipotii,
watamalizwa[d] kwa
silaha,[e]
Nao watakata pumzi bila
ujuzi.
13 Na wale walio waasi-imani
moyoni wataweka
hasira.[f]
Hawapaswi kulia wapewe
msaada kwa sababu
amewafunga.
14 Nafsi yao itakufa katika
ujana,[g]
Na uzima wao katikati
ya wanaume walio
makahaba wa hekaluni.[h]
15 Atamwokoa mwenye
kuteseka katika mateso
yake,
Naye atafungua sikio lao
katika ukandamizaji huo.
16 Naye hakika pia
atakushawishi kutoka
katika kinywa cha
taabu![i]
Mahali penye nafasi,[j] wala
si penye kufinyana,
patakuwa badala yake,
Na faraja ya meza yako
itajaa unono.[k]
17 Wewe hakika utajaa
adhabu ya hukumu juu
ya mwovu;[l]
Adhabu ya hukumu na
haki zitathibitika.

18 Ili uwe mwangalifu
kwamba ghadhabu[a]
isikushawishi upige
makofi ya chuki,
Wala usiache fidia[b] kubwa
ikupotoshe.
19 Je, kilio chako cha kuomba
msaada kitakuwa na
matokeo?[c] Hapana, wala
katika taabu
Hata jitihada zako zote
zenye nguvu.[d]
20 Usipumue kwa kutamani
usiku,
Wakati watu wanaporudi
kutoka mahali walipo.
21 Jilinde usigeukie jambo
lenye kudhuru,[e]
Kwa maana umelichagua
hilo badala ya mateso.[f]
22 Tazama! kwa nguvu
zake, Mungu mwenyewe
hutenda kwa njia
iliyoinuliwa;
Ni nani aliye mfundishaji
kama yeye?
23 Ni nani amemtaka atoe
hesabu juu ya njia yake,[g]
Na ni nani amesema,
'Wewe umetenda ukosefu
wa uadilifu'?[h]
24 Kumbuka kwamba
unapaswa kutukuza
utendaji wake[i]
Ambao wanadamu
wameimba juu yake.[j]
25 Wanadamu wote
wameutazama;
Mwanadamu anayeweza
kufa anaendelea
kutazama toka mbali.[k]
26 Tazama! Mungu
ameinuliwa sana kuliko
tunavyoweza kujua;[l]
Hesabu ya miaka yake
haichunguziki.[m]
27 Kwa maana yeye huyateka
matone ya maji;[n]
Yanajichuja kama mvua
yawe ukungu wake,
28 Hivi kwamba mawingu
yanadondoka,[a]
Yanadondoka kwa wingi
juu ya wanadamu.
29 Kwa kweli, ni
nani anayeweza kuelewa
tabaka za mawingu,
Mngurumo kutoka katika
kibanda chake?[b]
30 Tazama! Ametandaza juu
yake nuru yake,[c]
Naye ameifunika mizizi ya
bahari.
31 Kwa maana kwa hizo yeye
hutetea kesi ya vikundi
vya watu;[d]
Hutoa chakula kwa wingi.[e]
32 Amefunika umeme katika
mikono yake,
Naye huweka amri
juu yake dhidi ya
mshambuliaji.[f]
33 Kunguruma[g] kwake
hueleza habari zake,
Mifugo pia kuhusu yule
anayekuja.

37 "Kwa kweli moyo wangu
unaanza kutetemeka[h]
kutokana na hilo,
Nao unaruka kutoka
mahali pake.
2 Ninyi sikilizeni kwa
makini, mngurumo wa
sauti yake,[i]
Na mvumo unaotoka
kinywani mwake.
3 Anaiachilia iende chini ya
mbingu zote,
Na umeme[j] wake unafika
kwenye miisho ya dunia.
4 Nyuma yake sauti huvuma;
Yeye ananguruma[k] kwa
sauti ya ukuu wake,[l]
Naye hazizuii wakati sauti
yake inaposikiwa.[m]

SURA 36
a Met 19:19
Met 29:22
b Zb 49:7
c Eze 8:18
d Ayu 34:20
Zb 33:16
Met 11:4
e Zb 66:18
f Ebr 11:25
g Isa 40:14
h Ayu 34:10
Ro 9:14
i Zb 92:5
Zb 104:24
j Kut 15:1
Ufu 15:3
k Kut 20:18
l Zb 145:3
Zb 148:13
Ufu 10:6
Ufu 15:3
m Zb 90:2
Zb 102:27
1Ti 1:17
Ebr 1:12
n Mwa 2:6
Amo 5:8

Safu ya 2
a Kum 32:2
Met 3:20
Isa 55:10
Yer 14:22
b 2Sa 22:12
c Ayu 37:3
Mt 24:27
d Kut 9:23
Yos 10:11
Ayu 37:13
Ayu 38:23
e Mdo 14:17
f 2Sa 22:15
Zb 18:14
Zb 144:6
g 1Fa 18:41

SURA 37
h 1Sa 28:5
i Ayu 38:1
j Ayu 37:11
Zb 97:4
Lu 17:24
k Ayu 40:9
Zb 29:3
l Zb 148:13
m Zb 68:33

5 Mungu hunguruma kwa
sauti[a] yake kwa njia ya
ajabu,
Akifanya mambo makuu
ambayo hatuwezi kujua.[b]
6 Kwa maana yeye
anaiambia theluji,
'Anguka kuelekea
duniani,'[c]
Na pia mvua kubwa, ndiyo,
mvua zake kubwa zenye
nguvu.[d]
7 Anaweka muhuri juu ya
mkono wa kila mtu wa
udongo
Ili kila mwanadamu
anayeweza kufa ajue kazi
yake.
8 Na mnyama-mwitu huingia
katika mavizio,
Naye anakaa katika
maficho yake.[e]
9 Upepo wa dhoruba unatoka
katika chumba cha
ndani[f]
Na baridi kutoka katika
pepo za kaskazini.[g]
10 Barafu inaletwa kwa
pumzi ya Mungu[h]
Na upana wa maji uko chini
ya kizuizi.[i]
11 Ndiyo, yeye hubebesha
wingu mzigo wa
umajimaji,
Nuru[j] yake hutawanya
wingu kubwa,
12 Nalo linageuzwa huku na
huku kwa uongozi wake
ili yatende
Popote anapoyaamuru[k] juu
ya uso wa nchi yenye
kuzaa ya dunia.
13 Iwe ni kwa fimbo[l] au ni kwa
nchi yake[m]
Au ni kwa fadhili zenye
upendo,[n] hulifanya liwe
na matokeo.
14 Tega sikio kwa jambo hili,
Ee Ayubu;
Simama tuli na ukazie
fikira kazi za ajabu za
Mungu.[a]
15 Je, unajua wakati Mungu
alipoziagiza,[b]
Na wakati alipofanya nuru
ya wingu lake iangaze?
16 Je, unajua habari za kuelea
kwa wingu,[c]
Kazi za ajabu zake Yeye
aliye mkamilifu katika
ujuzi?[d]
17 Jinsi mavazi yako yalivyo
na moto
Wakati dunia
inapoonyesha utulivu
kutoka upande wa
kusini?[e]
18 Je, unaweza kutandaza
anga[f] pamoja na yeye
Iwe ngumu kama kioo cha
kuyeyushwa?
19 Tujulishe yale
tunayopaswa
kumwambia;
Hatuwezi kutokeza
maneno kwa sababu ya
giza.
20 Je, yeye ajulishwe kwamba
nataka kusema?
Au, je, mtu yeyote
amesema kwamba jambo
hilo lijulishwe?[g]
21 Na sasa kwa kweli
hawaioni nuru;
Ni nyangavu angani,
Upepo ukiisha kupita na
kuisafisha.
22 Fahari ya dhahabu huja
kutoka kaskazini.
Utukufu[h] ulio juu ya
Mungu ni wenye
kuogopesha.
23 Na kumhusu Mweza-Yote,
sisi hatujamjua;[i]
Yeye ameinuliwa katika
nguvu,[j]
Naye hatapuuza[k] haki[l] na
wingi wa uadilifu.[m]

SURA 37

a 2Sa 22:14
b Mhu 3:11
Ufu 15:3
c Zb 147:16
Isa 55:10
d Amo 9:6
e Zb 104:22
f Zb 104:3
g Met 25:23
h Ayu 38:29
Zb 147:16
i Ayu 26:8
Ayu 28:25
Ayu 38:30
j Ayu 37:3
k Zb 148:8
l Kut 9:23
1Sa 12:18
Ayu 36:31
m Ayu 38:27
n 1Fa 18:45
Yak 5:18

Safu ya 2

a Zb 111:2
Zb 145:5
b Ayu 38:4
c Ayu 36:29
d Ayu 36:4
Zb 18:30
Zb 104:24
e Lu 12:55
f Isa 44:24
g Ro 11:34
h 1Nya 16:27
1Nya 29:11
Zb 8:1
i Zb 145:3
Mhu 3:11
Ro 11:33
j 1Nya 29:11
Ayu 36:22
Isa 40:26
k Mdo 10:35
l Kum 32:4
Zb 33:5
Zb 37:28
m Zb 11:7
Zb 71:19

24 Kwa hiyo wanadamu na wamwogope.[a]
Yeye hawaangalii wowote walio na hekima katika moyo wao wenyewe.”[b]

38 Naye Yehova akaanza kumjibu Ayubu kutoka katika dhoruba ya upepo,[c] akasema:

2 “Ni nani huyu anayefunika shauri
Kwa maneno yasiyo na ujuzi?[d]
3 Tafadhali jifunge viuno vyako, kama mwanamume,
Na acha mimi nikuulize maswali, nawe unijulishe.[e]
4 Ulikuwa wapi nilipoweka msingi wa dunia?[f]
Niambie, ikiwa unaelewa.
5 Ni nani aliyeweka vipimo vyake, ikiwa unajua,
Au ni nani aliyenyoosha juu yake kamba ya kupimia?
6 Vikalio[g] vyake vimeingizwa ndani ya nini,
Au ni nani aliyeweka jiwe lake la pembeni,
7 Nyota za asubuhi[h] zilipopiga vigelegele pamoja kwa shangwe,
Na wana wote wa Mungu[i] wakaanza kupaaza sauti kwa kushangilia?
8 Na ni nani aliyeizuia bahari kwa milango,[j]
Iliyoanza kwenda kama katika wakati ilipotoka katika tumbo la uzazi;
9 Nilipoliweka wingu liwe vazi lake
Na giza zito liwe utepe wake wa kufungia,
10 Nami nikaweka sharti langu juu yake
Na kuweka pingo na milango,[a]
11 Nami nikasema, ‘Unaweza kufika hapa, na usipite;[b]
Na hapa mawimbi yako yenye fahari yamewekewa mpaka’?[c]
12 Je, uliiamuru asubuhi[d] tangu siku zako na kuendelea?
Je, uliyajulisha mapambazuko mahali pake,
13 Yapate kushika miisho ya dunia,
Ili waovu wakung’utwe kutoka ndani yake?[e]
14 Hujigeuza kama udongo[f] chini ya muhuri,
Na vitu husimama mahali pake kama katika mavazi.
15 Na nuru yake huzuiwa isiwafikie waovu,[g]
Na mkono ulio juu huvunjwa.[h]
16 Je, umeingia katika chemchemi za bahari,
Au, je, umetembea huku na huku[i] ukitafuta kilindi cha maji?[j]
17 Je, wewe umefunuliwa malango ya kifo,[k]
Au, je, unaweza kuona malango ya kivuli kizito?[l]
18 Je, umezifikiria kwa akili nafasi pana za dunia?[m]
Sema, kama umeyajua hayo yote.
19 Basi sasa, iko wapi njia inayoenda mahali ambapo nuru hukaa?[n]
Sasa nalo giza, mahali pake ni wapi,
20 Ili ulipeleke kwenye mpaka wake

SURA 37
a Zb 33:8; Met 1:7; Mt 10:28
b Met 3:7; Mt 11:25; Ro 11:20; Ro 12:16; 1Ko 1:26

SURA 38
c Kut 19:16; 1Fa 19:11
d Ayu 42:3; 1Ti 1:7
e Ayu 40:7
f Mwa 1:1; Ne 9:6; Zb 104:5; Zb 136:6; Met 8:29; Ebr 1:10
g Zb 104:5
h Ufu 22:16
i Mwa 6:2; 1Fa 22:19; Ayu 1:6; Ayu 2:1; Zb 89:6; Zb 104:4
j Zb 33:7; Met 8:29; Mdo 4:24

Safu ya 2
a Mwa 1:9; Yer 5:22
b Met 8:29
c Zb 89:9
d Mwa 1:5; Zb 74:16; Zb 148:5
e Ayu 24:15; 1Th 5:7
f Yer 18:6
g Kut 10:21; Ayu 33:30
h Zb 10:15; Yer 48:25; Eze 30:22
i Zb 77:19
j Mwa 1:2
k Zb 9:13; Zb 107:18; Mt 16:18; Ufu 1:18
l Ayu 10:21
m Zb 74:17; Zb 89:11
n Isa 45:7

Na ili uzielewe barabara
zinazoenda katika
nyumba yake?
21 Je, umepata kujua kwa
sababu wakati huo
ulikuwa ukizaliwa,[a]
Na kwa sababu hesabu ya
siku zako ni nyingi?
22 Je, umeingia katika
maghala ya theluji,[b]
Au, je, unayaona hata
maghala ya mvua ya
mawe,[c]
23 Ambayo nimeyaweka kwa
ajili ya wakati wa msiba,
Kwa ajili ya siku ya pigano
na vita?[d]
24 Basi sasa, iko wapi njia
ambayo katika hiyo nuru
hujigawanya,
Na ambayo upepo wa
mashariki[e] hutawanyika
huku na huku juu ya
dunia?
25 Ni nani ameugawanya
mfereji kwa ajili ya
mafuriko
Na njia kwa ajili ya
wingu la dhoruba lenye
kunguruma,[f]
26 Ili kulifanya linyeshe juu
ya nchi isiyokuwa na
mwanadamu,[g]
Juu ya nyika isiyokuwa na
mtu wa udongo,
27 Ili kushibisha maeneo
yenye kupigwa na
dhoruba na yenye ukiwa
Na kusababisha majani
kuchipuka?[h]
28 Je, mvua[i] ina baba,
Au ni nani aliyezaa matone
ya umande?[j]
29 Kwa kweli barafu hutoka
katika tumbo la nani,
Nayo sakitu[k] ya mbinguni,
ni nani hasa anayeizaa?
30 Maji hujificha kana
kwamba ni katika jiwe,

SURA 38
a Ayu 38:12
b Ayu 6:16
Ayu 37:6
c Yos 10:11
Isa 30:30
d Kut 9:24
Eze 13:13
e Zb 78:26
Zb 135:7
f Ayu 28:26
g Zb 104:13
Zb 107:35
h 2Sa 23:4
Zb 147:8
Ebr 6:7
i 1Sa 12:18
Isa 30:23
Yer 5:24
j Mwa 27:28
k Zb 147:16

Safu ya 2
a Ayu 37:10
b Amo 5:8
c Met 3:19
Yer 31:35
Yer 33:25
d Zek 10:1
e Yer 10:12
f Zb 136:5
Met 3:20
g Yer 10:13

Na uso wa kilindi cha maji
hujigandisha.[a]
31 Je, unaweza kufunga
vifungo vya kundi-nyota
la Kima,
Au, je, unaweza kufungua
kamba za kundi-nyota la
Kesili?[b]
32 Je, unaweza kuleta
kundi-nyota la
Mazarothi katika wakati
wake uliowekwa?
Na kwa habari
ya kundi-nyota la Ashi,
je, unaweza kuliongoza
pamoja na wanawe?
33 Je, umepata kujua sheria
za mbingu,[c]
Au, je, unaweza kutia amri
yake duniani?
34 Je, unaweza kulipaazia
wingu sauti yako,
Ili maji mengi
yanayosukasuka
yakufunike?[d]
35 Je, unaweza kuutuma
umeme ili uende
Na kukuambia, ‘Sisi tupo
hapa!’?
36 Ni nani aliyetia hekima[e]
katika tabaka za
mawingu,
Au ni nani aliyeyapa
uelewaji[f] maajabu ya
angani?
37 Ni nani anayeweza
kuhesabu kwa ukamili
mawingu kwa hekima,
Au mitungi ya maji
ya mbingu—ni nani
anayeweza kuipindua,[g]
38 Wakati mavumbi
yanapomwagika kana
kwamba ni fungu
lililoyeyushwa,
Na madonge ya udongo
kushikamana?
39 Je, unaweza kumwindia
simba mawindo

Na, je, unaweza kuishibisha
hamu kubwa ya
wana-simba,[a]
40 Wanapochutama
mafichoni,[b]
Au wanapoendelea kujilaza
katika maficho ya
kuvizia?
41 Ni nani anayemtayarishia
kunguru chakula chake[c]
Wakati watoto wake
wanapomlilia Mungu
wapate msaada,
Wanapoendelea
kutanga-tanga kwa
sababu hakuna chakula
chochote?

39 "Je, umepata kujua
wakati uliowekwa wa
mbuzi wa milimani
kuzaa?[d]
Je, unaangalia wakati ule
paa wanapozaa[e] kwa
uchungu?
2 Je, wewe huhesabu miezi
ambayo wao hutimiza,
Au, je, umepata
kujua wakati uliowekwa
ambapo wao huzaa?
3 Wao huinama wanapotoa
watoto wao,
Wanapoondoa uchungu
wao.
4 Wana wao huwa wenye
nguvu, huwa wakubwa
porini;
Kwa kweli wao huenda zao
wala hawarudi kwao.
5 Ni nani aliyemwachilia
punda-milia[f] awe huru,
Na ni nani
aliyevifungua vifungo
vya punda-mwitu,
6 Ambao nimeweka nchi
tambarare ya jangwa
kuwa nyumba yao
Na ambao makao yao ni
nchi ya chumvi?[g]

SURA 38
a Zb 104:21
Zb 145:15
Nah 2:12
b Omb 3:10
c Zb 104:27
Zb 147:9
Mt 6:26
Lu 12:24

SURA 39
d Zb 104:18
e Zb 29:9
f Ayu 24:5
Zb 104:11
g Kum 29:23
Yer 17:6

Safu ya 2
a Ayu 3:18
b Ayu 40:20
c Mwa 1:30
Ayu 40:15
d Hes 23:22
Kum 33:17
Zb 29:6
e Isa 28:24
f Zb 104:17
Zek 5:9
g Omb 4:3

7 Yeye huyacheka
machafuko ya mji;
Naye hasikii kelele za
mwindaji.[a]
8 Yeye hutafuta-tafuta
malisho yake milimani[b]
Naye hutafuta kila namna
ya mmea wa kijani.[c]
9 Je, ng'ombe-mwitu hutaka
kukutumikia,[d]
Au, je, atalala usiku
kwenye hori yako?
10 Je, utamfunga imara
ng'ombe-mwitu kwa
kamba zake katika
mtaro,
Au, je, yeye atalima[e]
nchi tambarare za chini
nyuma yako?
11 Je, utamtegemea kwa
kuwa ana nguvu nyingi,
Na, je, utamwachia yeye
kazi yako ngumu?
12 Je, utamtegemea kwamba
atarudisha mbegu zako
Na kwamba atakusanya
kwenye uwanja wako wa
kupuria?
13 Je, bawa la mbuni-jike
limepiga-piga kwa
shangwe,
Au, je, yeye ana mbawa za
korongo[f] na manyoya?
14 Kwa maana yeye huyaacha
mayai yake katika nchi
Naye huyatia joto katika
mavumbi,
15 Naye husahau kwamba
mguu fulani unaweza
kuyavunja
Au hata mnyama
wa mwituni anaweza
kuyakanyaga.
16 Yeye huwatendea wanawe
kwa ukali, kana kwamba
si wake[g]—
Kazi yake ngumu ni ya
ubatili kwa sababu yeye
hana hofu.

17 Kwa maana Mungu
amemfanya asahau
hekima,
Naye hakumpa fungu
katika uelewaji.[a]
18 Wakati anapopiga-piga
mabawa yake juu,
Yeye humcheka farasi na
mpandaji wake.
19 Je, unaweza kumpa farasi
nguvu?[b]
Je, unaweza kuivika
shingo yake manyoya
yanayotetema?
20 Je, unaweza kumfanya
aruke kama nzige?
Fahari ya kukoroma kwake
ni yenye kutisha.[c]
21 Yeye huparapara[d] katika
nchi tambarare ya chini
na kufurahia nguvu;
Husonga mbele kukutana
na silaha.[e]
22 Huicheka hofu, naye
hatishiki;[f]
Wala harudi nyuma kwa
sababu ya upanga.
23 Podo hupiga kelele juu yake,
Kichwa cha mkuki na pia
fumo.
24 Yeye huimeza nchi kwa
mwendo wa kishindo na
msisimuko,
Wala haamini kwamba ni
sauti ya baragumu.
25 Mara tu baragumu
inapopiga yeye husema
Aha!
Naye hunusa harufu ya
pigano kutoka mbali sana,
Mshindo wa wakuu na
kelele za vita.[g]
26 Je, ni kwa sababu ya
uelewaji wako kwamba
kipanga hupaa juu,
Kwamba yeye hunyoosha
mabawa yake kuuelekea
upepo wa kusini?
27 Au, je, ni kwa agizo lako
kwamba tai[a] huruka
kuelekea juu
Na kwamba hujenga kiota
chake huko juu,[b]
28 Kwamba yeye hukaa
kwenye mwamba na
wakati wa usiku hukaa
Juu ya ncha ya mwamba
na mahali pasipoweza
kufikiwa?
29 Kutoka hapo yeye hutafuta
chakula;[c]
Macho yake huendelea
kutazama mbali sana.
30 Na watoto wake huendelea
kunywa damu;
Na mahali walipo wale
waliouawa, yeye yupo
hapo."[d]

40 Naye Yehova akaendelea
kumjibu Ayubu, akasema:
2 "Je, inampasa mtu
anayetafuta makosa
kushindana na
Mweza-Yote?[e]
Mwenye kumkaripia
Mungu na ajibu hayo
yeye mwenyewe."[f]
3 Naye Ayubu akamjibu Yehova, akasema:
4 "Tazama! Nimekuwa kitu
kisicho na maana.[g]
Nitakujibu nini?
Nimeuweka mkono wangu
juu ya kinywa changu.[h]
5 Nimesema mara moja,
nami sitajibu;
Na mara mbili, nami
sitaongeza lolote."
6 Na Yehova akaendelea kumjibu Ayubu kutoka katika ile dhoruba ya upepo,[i] akasema:
7 "Tafadhali, jifunge
viuno vyako, kama
mwanamume;[j]
Nitakuuliza maswali, nawe
unijulishe.[k]

SURA 39
a Ayu 35:11
b Zb 147:10
Isa 31:1
c Yer 8:16
d Amu 5:22
Zb 32:9
Yer 47:3
Hab 1:8
e Met 21:31
Yer 46:9
f Isa 5:28
Yer 8:6
g Yer 46:4
Amo 1:14

Safu ya 2
a Met 23:5
Isa 40:31
b Yer 49:16
Oba 4
c Ayu 9:26
Yer 49:22
d Mt 24:28

SURA 40
e Ayu 21:15
Ayu 33:13
Isa 45:9
Ufu 4:8
f Ayu 13:3
Ayu 23:4
Ayu 31:35
Ro 9:19
g Ezr 9:6
Ayu 42:6
Zb 51:4
h Amu 18:19
Ayu 29:9
Zb 39:9
Met 30:32
i Ayu 38:1
j Ayu 38:3
k Ayu 42:4

8 Kwa kweli, je, utaifanya
haki yangu kuwa bure?
Je, utanitangaza mimi
kuwa mwovu ili wewe
uwe upande wa haki?[a]
9 Au, je, una mkono kama
ule wa Mungu wa kweli,[b]
Na, je, unaweza kutoa
mngurumo kwa sauti
kama yake?[c]
10 Tafadhali, jipambe kwa
ukuu[d] na ustahiki;[e]
Nawe ujivike utukufu[f] na
fahari.[g]
11 Milipuko mikali ya hasira
yako na imwagike,[h]
Na uone kila mtu mwenye
majivuno na umshushe
chini.
12 Mwone kila mtu mwenye
majivuno, mnyenyekeze,[i]
Na uwakanyagie chini
waovu palepale walipo.
13 Wafiche pamoja katika
mavumbi,[j]
Funga nyuso zao katika
mahali palipofichika,
14 Nami, naam, mimi
nitakupongeza,
Kwa sababu mkono wako
wa kuume unaweza
kukuokoa.
15 Tazama, sasa, Behemothi*
ambaye nimemfanya na
wewe pia.
Yeye hula majani[k] kama
ng'ombe.
16 Tazama, basi, nguvu zake
zimo katika viuno vyake,
Na nishati[l] zake zimo
katika kano za tumbo
lake.
17 Yeye huinamisha mkia
wake kama mwerezi;
Kano za mapaja yake
zimeungamana pamoja.
18 Mifupa yake ni mianzi ya
shaba;
Mifupa yake yenye nguvu
ni kama fimbo za chuma
iliyofuliwa.
19 Yeye ni mwanzo wa njia za
Mungu;
Mtengenezaji[a] wake
anaweza kuleta karibu
upanga wake.
20 Kwa maana milima
yenyewe humzalia mazao
yake,[b]
Na wanyama wote wa
mwituni hucheza huko.
21 Yeye hulala chini
ya miyungiyungi yenye
miiba,
Katika mahali
palipofichika penye
matete[c] na mahali penye
majimaji.[d]
22 Miyungiyungi yenye miiba
humzuia kwa kivuli
chake;
Mierebi ya bonde la mto
humzunguka.
23 Mto ukitenda kwa jeuri,
yeye hakimbii kwa
wasiwasi.
Ana uhakika, hata Yordani[e]
ukifurika juu ya kinywa
chake.
24 Je, yeyote anaweza
kumshika akiwa anaona?
Je, yeyote anaweza
kuitoboa pua yake kwa
mitego?

41 "Je, unaweza kumvua
Lewiathani*[f] kwa
ndoano,
Au, je, unaweza
kuufunga ulimi wake
kwa kamba?
2 Je, unaweza kutia kitete
katika pua yake,[g]
Au, je, unaweza kutoboa
taya zake kwa mwiba?

SURA 40
a Zb 51:4
Ro 3:4
b Kut 15:6
Zb 89:13
1Ko 10:22
c Ayu 37:4
Zb 29:3
d Isa 2:10
Isa 24:14
e Zb 83:18
f 1Nya 16:27
Zb 8:1
g Zb 104:1
h Zb 78:49
Zb 90:11
Yer 30:23
i 2Sa 22:28
Zb 18:27
Met 15:25
Isa 2:11
Da 4:37
j Zb 49:14
Zb 55:15
k Mwa 1:30
Zb 104:14
l Isa 40:26

Safu ya 2
a Zb 104:24
b Zb 104:14
c Zb 68:30
Isa 19:6
d Ayu 8:11
e Yos 3:15

SURA 41
f Ayu 3:8
Zb 104:26
g Isa 37:29

Ayu 40:15* Au kiboko.

Ayu 41:1* Au mamba.

3 Je, atakusihi wewe sana,
Au, je, atakuambia maneno
ya upole?
4 Je, atafanya agano pamoja
nawe,
Ili umfanye kuwa mtumwa
mpaka wakati usio na
kipimo?
5 Je, utamchezea kama
ndege,
Au, je, utamfunga kwa
ajili ya wasichana wako
wadogo?
6 Je, rafiki watafanya
biashara juu yake?
Je, watamgawanya
yeye katikati ya
wafanya-biashara?
7 Je, utajaza vyuma vyenye
ncha[a] katika ngozi yake,
Au kujaza mikuki ya
samaki katika kichwa
chake?
8 Tia mkono wako juu yake.
Kumbuka pigano hilo.
Usifanye hivyo tena.
9 Tazama! Matarajio ya
mtu kumhusu hakika
yatakatishwa tamaa.
Mtu pia ataangushwa chini
kwa kule kumwona tu.
10 Hakuna aliye na ushupavu
kiasi cha kumwamsha.
Na ni nani ambaye anaweza
kusimama mbele zangu?[b]
11 Ni nani ambaye
amenipa kitu kwanza,
ndipo nilazimike kumpa
thawabu?[c]
Vitu vyote ni vyangu chini
ya mbingu zote.[d]
12 Sitanyamaza kimya
kuhusu sehemu zake
Au habari ya nguvu zake
na uzuri wa vipimo
vyake.
13 Ni nani ambaye ameufunua
uso wa mavazi yake?

SURA 41

a Ayu 41:26

b 2Nya 20:6
Da 4:35
Mdo 11:17
Ro 9:19

c Ro 11:35

d Kut 19:5
Kum 10:14
Zb 24:1
Zb 50:12
1Ko 10:26

Ni nani anayeweza
kuingia ndani ya taya
zake mbili?
14 Ni nani amepata kuifungua
milango ya uso wake?
Meno yake kuzunguka
pande zote ni yenye
kuogopesha.
15 Mitaro ya magamba ndiyo
majivuno yake,
Yaliyofungwa kana
kwamba kwa muhuri
uliokazwa.
16 Hayo huingiana yenyewe
karibu-karibu,
Na hata hewa haiwezi
kuingia katikati yake.
17 Yamefungamana kila moja
na lingine;
Yanashikamana wala
hayawezi kutenganishwa.
18 Chafya zake huangaza
nuru,
Na macho yake ni kama
miali ya mapambazuko.
19 Miwako ya umeme hutoka
katika kinywa chake,
Hata cheche za moto
hutoka.
20 Moshi hutoka katika
mianzi ya pua yake,
Kama tanuru iliyowashwa
moto kwa matete.
21 Nafsi yake huwasha moto
makaa,
Na mwali wa moto hutoka
katika kinywa chake.
22 Nguvu zinakaa katika
shingo yake,
Na ukataji tamaa hukimbia
mbele yake.
23 Makunjo ya nyama yake
hushikamana pamoja;
Hayo ni kama
kitu kilichoundwa katika
kalibu juu yake,
kisichoondoleka.
24 Moyo wake umetengenezwa
kama jiwe,

Ndiyo, umetengenezwa
kama jiwe la chini la
kusagia.
25 Wenye nguvu huingiwa na
woga kwa sababu ya
kuinuka kwake;[a]
Wao hutatanishwa na
fadhaa.
26 Upanga ukimfikia
haumwezi,
Wala mkuki, kishale wala
ncha ya mshale.[b]
27 Yeye huona chuma[c] kuwa
kama nyasi tu,
Shaba kuwa kama mti
uliooza.
28 Mshale haumfukuzi;
Kwake mawe ya kombeo[d]
yamebadilishwa kuwa
majani makavu.
29 Yeye huiona rungu kuwa
kama tu majani makavu,[e]
Naye huucheka mtikiso wa
mkuki.
30 Sehemu zake za chini
ni kama vigae
vilivyochongoka;
Yeye hujinyoosha kama
kifaa cha kupuria[f] juu ya
matope.
31 Yeye huvichemsha vilindi
kama chungu;
Huifanya bahari iwe kama
chungu cha marhamu.
32 Hufanya njia ing'ae nyuma
yake;
Mtu atafikiri kilindi cha
maji ni kichwa chenye
mvi.
33 Hakuna aliye kama yeye
juu ya mavumbi,
Yeye aliyefanywa asiweze
kutishika.
34 Yeye huona kila kitu
kilicho juu.
Yeye ni mfalme juu
ya wanyama-mwitu wote
wenye fahari."

SURA 41
a Ayu 41:9
b Ayu 41:7
c Yos 17:16
d Amu 20:16
2Nya 26:14
e Met 25:18
Eze 9:2
f Isa 41:15

Safu ya 2

SURA 42
a Mwa 18:14
Isa 43:13
Yer 32:17
Mk 10:27
Lu 18:27
b Zb 135:6
Isa 55:11
c Ayu 38:2
d Zb 40:5
Zb 131:1
Zb 139:6
e Ayu 38:3
Ayu 40:7
f Ezr 9:6
Ayu 40:4
Zb 51:17
g Ayu 2:11
h Ayu 11:6
Ayu 15:15
Ayu 22:2
i Hes 23:1
j Mt 5:24
k Mwa 20:17
Yak 5:15

42 Naye Ayubu akamjibu
Yehova, akasema:
2 "Nimepata kujua kwamba
unaweza kufanya mambo
yote,[a]
Wala hakuna wazo lolote
ambalo huwezi kulifikia.[b]
3 'Ni nani huyu anayefunika
shauri bila ujuzi?'[c]
Kwa hiyo nilisema, lakini
sikuwa ninaelewa
Mambo yaliyo ya ajabu mno
kwangu, ambayo siyajui.[d]
4 'Sikia, tafadhali, nami
mwenyewe nitasema.
Nitakuuliza maswali, nawe
unijulishe.'[e]
5 Nimesikia habari zako kwa
fununu,
Lakini sasa jicho langu
mwenyewe linakuona
wewe.
6 Ndiyo sababu ninayatangua
niliyosema,
Nami ninatubu[f] katika
mavumbi na majivu."
7 Na ikawa baada ya Yeho-
va kumwambia Ayubu maneno
hayo, ndipo Yehova akamwa-
mbia Elifazi Mtemani:
"Hasira yangu imewaka juu
yako na rafiki zako wawili,[g] kwa
maana ninyi hamkusema ma-
mbo ya kweli[h] kunihusu mimi
kama mtumishi wangu Ayu-
bu. **8** Na sasa chukueni ng'o-
mbe-dume saba[i] na kondoo-
dume saba[j] kisha mwende kwa
mtumishi wangu Ayubu, na-
nyi mtoe dhabihu ya kutekete-
zwa kwa ajili yenu wenyewe; na
Ayubu mtumishi wangu atasali
kwa ajili yenu.[k] Nitakubali uso
wake peke yake ili nisiwatendee
ninyi upumbavu wenye kufe-
dhehesha, kwa maana hamku-
sema mambo ya kweli kunihusu

mimi, kama mtumishi wangu Ayubu."[a]

9 Basi Elifazi Mtemani na Bildadi Mshua na Sofari Mnaamathi wakaenda, wakafanya kama Yehova alivyowaambia; na kwa hiyo Yehova akaukubali uso wa Ayubu.

10 Na Yehova akaigeuza hali ya mateka ya Ayubu[b] aliposali kwa ajili ya wale rafiki zake,[c] na Yehova akaanza kumpa na kumwongezea Ayubu vyote vilivyokuwa vyake, kiasi cha mara mbili.[d] **11** Na ndugu zake wote na dada zake wote na wale wote waliokuwa wakimjua[e] hapo mwanzoni wakaendelea kuja kwake, nao wakaanza kula mkate pamoja naye[f] katika nyumba yake na kusikitika pamoja naye na kumfariji juu ya msiba wote ambao Yehova alikuwa ameuruhusu uje juu yake; nao wakaanza kila mmoja wao kumpa kipande cha pesa na kila mmoja pete ya dhahabu.

12 Naye Yehova akaubariki[a] mwisho wa Ayubu baadaye kuliko mwanzo wake,[b] hivi kwamba akawa na kondoo kumi na nne elfu na ngamia elfu sita na jozi elfu moja za ng'ombe na punda-jike elfu moja. **13** Pia akawa na wana saba na binti watatu.[c] **14** Naye akamwita yule wa kwanza jina Yemima na yule wa pili Kezia na yule wa tatu Kereni-hapuku. **15** Na hapakuonekana wanawake wowote walio warembo kama wale binti za Ayubu katika nchi yote, na baba yao akawapa urithi katikati ya ndugu zao.[d]

16 Naye Ayubu akaendelea kuishi miaka 140[e] baada ya mambo hayo, akaona wanawe na wajukuu wake[f]—vizazi vinne. **17** Na mwishowe Ayubu akafa, akiwa mzee na mwenye kushiba siku.[g]

SURA 42
a Ayu 42:7 Met 6:17
b Ayu 2:6 Yak 5:11
c Mt 6:14
d Mwa 32:10 1Sa 2:7 2Nya 25:9 Met 22:4 Isa 61:7
e Ayu 19:13
f Met 24:29 Ro 12:15

Safu ya 2
a Met 3:33 Met 10:22 Ebr 11:6 Yak 5:11
b Ayu 1:3 Mhu 7:8
c Ayu 1:2
d Yos 15:19
e Met 3:16
f Zb 128:6
g Mwa 25:8

ZABURI

KITABU CHA KWANZA
(Zaburi 1 – 41)

1 Mwenye furaha[a] ni mtu
ambaye hakutembea
katika shauri la waovu,[b]
Na katika njia ya
watenda-dhambi
hakusimama,[c]
Na katika kiti cha wenye
dhihaka hakuketi.[d]
2 Bali mapendezi yake ni
katika sheria ya Yehova,[e]
Naye huisoma sheria yake
kwa sauti ya chini
mchana na usiku.[f]
3 Naye hakika atakuwa
kama mti uliopandwa
kando ya vijito vya maji,[a]
Ambao hutoa matunda
yake katika majira yake[b]
Na ambao majani yake
hayanyauki,[c]
Na kila jambo analofanya
litafanikiwa.[d]

SURA 1
a Zb 112:1 Mt 5:3
b 2Nya 22:3 Ayu 21:16 Zb 64:2 Mt 26:4 Mdo 9:23
c Met 4:14
d Zb 26:4 Zb 69:12 Met 22:10 2Pe 3:3
e Zb 19:7 Zb 40:8 Ro 7:22 Yak 1:25
f Yos 1:8 Zb 35:28 Zb 119:97 1Ti 4:15

Safu ya 2 a Isa 44:4; Isa 61:3; Yer 17:8; b Mt 21:43; Flp 4:17; Ufu 22:2; c Isa 27:11; d Mwa 39:3; 1Nya 22:13.

4 Waovu hawako hivyo,
Bali wako kama
makapi ambayo upepo
hupeperusha.[a]
5 Ndiyo sababu waovu
hawatasimama katika
hukumu,[b]
Wala watenda-dhambi
katika kusanyiko la
waadilifu.[c]
6 Kwa maana Yehova anaijua
njia ya waadilifu,[d]
Bali njia ya waovu
itaangamia.[e]

2 Kwa nini mataifa
yamekuwa na fujo[f]
Na vikundi vya mataifa
vimeendelea kusema
jambo la upuuzi?[g]
2 Wafalme wa dunia
wanachukua
msimamo wao[h]
Nao maofisa wakuu
wamejikusanya pamoja
kama mtu mmoja[i]
Dhidi ya Yehova[j] na dhidi
ya mtiwa-mafuta wake,[k]
3 Wakisema: "Na tuzikate
pingu zao[l]
Na kuzitupa kamba zao
mbali nasi!"[m]
4 Yule anayeketi mbinguni[n]
atacheka;
Yehova mwenyewe
atawadharau.[o]
5 Wakati huo atasema nao
katika hasira yake[p]
Na katika ghadhabu yake
atawafadhaisha,[q]
6 Na kusema: "Mimi,
naam, mimi nimemweka
mfalme wangu[r]
Juu ya Sayuni,[s] mlima
wangu mtakatifu."[t]
7 Acheni nirejezee agizo la
Yehova;
Yeye ameniambia: "Wewe
ni mwanangu;[u]
Mimi, leo, nimekuwa baba
yako.[a]
8 Niombe,[b] ili nikupe mataifa
yawe urithi wako[c]
Na miisho ya dunia iwe
miliki yako mwenyewe.[d]
9 Utawavunja kwa fimbo ya
chuma ya enzi,[e]
Utawavunja
vipande-vipande, kama
chombo cha mfinyanzi."[f]
10 Na sasa, enyi wafalme,
onyesheni ufahamu;
Kubalini kurekebishwa,
enyi waamuzi wa dunia.[g]
11 Mtumikieni Yehova kwa
woga[h]
Na mshangilie kwa
kutetemeka.[i]
12 Mbusuni mwana,[j] ili
Yeye asikasirike
Nanyi msiangamizwe
kutoka njiani,[k]
Kwa maana hasira yake
huwaka kwa urahisi.[l]
Wenye furaha ni wale
wote wanaomkimbilia.[m]

Muziki wa Daudi alipokuwa akikimbia kwa sababu ya Absalomu mwana wake.[n]

3 Ee Yehova, kwa nini
adui zangu wamekuwa
wengi?[o]
Kwa nini wengi wanainuka
dhidi yangu?[p]
2 Wengi wanasema juu ya
nafsi yangu:
"Hakuna wokovu kwa
ajili yake kutoka kwa
Mungu."[q] *Sela*.
3 Na bado wewe, Ee Yehova,
ni ngao inayonizunguka,[r]

SURA 1

a Ayu 21:18 Zb 35:5 Isa 17:13 Mt 3:12
b Zb 5:5 Yud 15
c Mal 3:18 Mt 13:49 Mt 25:41
d Ayu 23:10 Zb 37:18 Yer 12:3 2Ti 2:19 1Pe 3:12
e Met 14:12

SURA 2

f Zb 46:6 Mt 24:7 Mdo 4:25
g Zb 33:10 Isa 40:15 Isa 60:2
h Zb 48:4 Lu 13:31 Lu 23:11 Ufu 19:19
i Mt 27:1 Mk 3:6
j Zb 83:5 Yoh 5:23 Yoh 15:24
k Zb 45:7 Zb 89:20 Isa 61:1 Mdo 4:27
l Lu 19:14
m Yer 5:5
n Zb 11:4 Zb 68:33
o Zb 37:13 Zb 59:8
p Zb 90:11 Yer 25:31 Nah 1:6
q Ebr 3:16
r Zb 45:6 Eze 17:22 Eze 21:27 Da 7:14 Yoh 1:49 Ufu 19:16
s 2Sa 5:7 Ebr 12:22 Ufu 14:1
t Isa 27:13
u 2Sa 7:14 Mt 3:17 Ro 1:4 Ebr 1:5 Ebr 5:5

Safu ya 2

a Zb 89:27 Mk 1:11 Yoh 1:14 Mdo 13:33
b Mt 28:18
c Zb 22:27 Zb 110:2 Mt 25:32
d Zb 72:8 Ebr 1:2 Ufu 11:15
e Ufu 2:27 Ufu 12:5 Ufu 19:15
f Da 2:44
g Zb 72:1 Zb 82:2
h Zb 19:9 Met 28:14 Flp 2:12 Ebr 12:28

i Zb 95:1; Zb 99:1; Zb 119:120; j Mwa 49:10; Lu 7:45; Flp 2:10; k Zb 1:6; Yoh 3:36; Yoh 14:6; l 2Th 1:9; Ufu 6:16; m Isa 11:10; Isa 32:2; Ro 9:33; **SURA 3** n 2Sa 15:14; o 2Sa 15:12; 2Sa 16:15; p 2Sa 12:11; q 2Sa 16:8; Zb 22:7; Mt 27:43; r Mwa 15:1; Kum 33:29.

Utukufu[a] wangu na
Mwenye kuinua
kichwa changu.[b]
4 Kwa sauti yangu
nitamwita Yehova,
Naye atanijibu kutoka
katika mlima wake
mtakatifu.[c] *Sela*.
5 Nami nitajilaza nipate
kulala usingizi;
Hakika nitaamka,
kwa maana Yehova
anaendelea
kunitegemeza.[d]
6 Sitaogopa maelfu kumi
ya watu
Ambao wamejipanga dhidi
yangu kunizunguka
pande zote.[e]
7 Usimame,[f] Ee Yehova!
Uniokoe,[g] Ee Mungu
wangu![h]
Kwa maana utawapiga
adui zangu wote
kwenye taya.[i]
Utayavunja meno ya
waovu.[j]
8 Wokovu ni wa Yehova.[k]
Baraka yako iko juu ya
watu wako.[l] *Sela*.

Kwa kiongozi wa vinanda.[m]
Muziki wa Daudi.

4 Ninapoita, unijibu,
Ee Mungu wangu
mwadilifu.[n]
Katika taabu unifanyie
nafasi pana
Nionyeshe kibali[o] na
kuisikia sala yangu.
2 Enyi wana wa
watu, utukufu[p] wangu
utatukanwa mpaka
wakati gani,
Huku mkiendelea kupenda
mambo ya upuuzi,
Huku mkiendelea kutafuta
uwongo? *Sela*.

SURA 3

a Isa 45:25
Yoh 1:14
b Mwa 40:13
Zb 27:6
c 2Sa 15:25
1Fa 8:30
1Fa 8:45
Zb 2:6
Isa 2:3
d Zb 4:8
Zb 127:2
Met 3:24
e 2Fa 6:15
Zb 27:3
Zb 121:7
Ro 8:31
f Zb 10:12
Isa 51:9
g Zb 109:26
Mt 27:43
1Ti 4:10
h Zb 35:23
Yoh 20:17
i Ayu 16:10
Ayu 29:17
j Zb 58:6
2Th 1:6
k Zb 37:39
Met 21:31
Isa 43:11
Ho 13:4
Yon 2:9
Ufu 19:1
l Zb 29:11
Efe 1:3
Ebr 6:14

SURA 4

m 1Nya 25:1
n Zb 11:7
Isa 45:24
Yer 23:6
o Zb 9:13
p Zb 3:3

Safu ya 2

a 1Sa 2:9
Met 2:8
b Zb 34:15
Zb 55:16
c Efe 4:26
d Zb 63:6
e Kum 33:19
Zb 51:19
f Zb 37:3
Zb 62:8
Met 3:5
1Pe 4:19
g Hes 6:26
Zb 80:7
Zb 89:15
Zb 119:135
Met 16:15
1Pe 3:12
h Ne 12:43
Isa 9:3
i Yer 48:33
j Zb 3:5
Met 3:24
k Law 25:18
Kum 12:10
Eze 34:25

SURA 5

l Zb 55:1
Zb 65:2
1Pe 3:12
m Zb 3:4
n Zb 44:4
Zb 74:12
Zb 145:1
Isa 33:22

3 Basi jueni kwamba hakika
Yehova atamtendea
mshikamanifu wake kwa
njia ya pekee;[a]
Yehova mwenyewe atasikia
ninapomwita.[b]
4 Fadhaikeni, lakini
msitende dhambi.[c]
Semeni moyoni mwenu,
kitandani mwenu,[d] na
kunyamaza. *Sela*.
5 Toeni dhabihu za uadilifu,[e]
Na kumtumaini Yehova.[f]
6 Kuna wengi
wanaosema: "Ni nani
atakayetuonyesha
mema?"
Inua nuru ya uso wako juu
yetu,[g] Ee Yehova.
7 Hakika wewe utaupa moyo
wangu shangwe[h]
Iliyo kubwa kuliko wakati
ambapo nafaka yao na
divai yao mpya imejaa.[i]
8 Katika amani nitajilaza
na kulala usingizi,[j]
Kwa maana wewe peke
yako, Ee Yehova,
hunifanya nikae kwa
usalama.[k]

Kwa kiongozi wa Nehilothi.
Muziki wa Daudi.

5 Kwa maneno yangu utege
sikio,[l] Ee Yehova;
Uelewe kuugua kwangu.
2 Sikiliza kwa makini sauti
ya kilio changu kwa
ajili ya msaada,[m]
Ee Mfalme[n] wangu na
Mungu wangu, kwa
maana kwako wewe
ninasali.[o]
3 Ee Yehova, asubuhi
utasikia sauti yangu;[p]
Asubuhi nitajieleza kwako
na kukaa macho.[q]

o Zb 65:2; Mt 6:9; p Zb 55:17; Zb 88:13; q Mk 1:35.

4 Kwa maana wewe si
Mungu anayependezwa
na uovu;[a]
Hakuna mtu yeyote mbaya
atakayekaa na wewe
kwa muda wowote.[b]
5 Hakuna watu wowote
wenye kujisifu
watakaosimama mbele
za macho yako.[c]
Wewe huwachukia wote
wanaozoea kufanya
mambo yenye kuumiza;[d]
6 Utawaangamiza wale
wanaosema uwongo.[e]
Mtu anayemwaga damu[f] na
mdanganyifu[g]
Yehova anamchukia.
7 Na mimi, katika wingi
wa fadhili zako zenye
upendo[h]
Nitaingia katika nyumba
yako,[i]
Nitainama kulielekea
hekalu lako takatifu
kwa kukuogopa.[j]
8 Ee Yehova, uniongoze
katika uadilifu[k] wako
kwa sababu ya adui
zangu;[l]
Uifanye njia yako iwe laini
mbele yangu.[m]
9 Kwa maana katika kinywa
chao hakuna lolote lenye
kutegemeka;[n]
Sehemu yao ya ndani ni
shida kwelikweli.[o]
Koo yao ni kaburi lililo
wazi;[p]
Wanatumia ulimi laini.[q]
10 Hakika Mungu
atawahesabia hatia;[r]
Wataanguka kwa sababu
ya mashauri yao
wenyewe.[s]
Na watawanywe katika
wingi wa makosa yao,[t]
Kwa sababu wamekuasi
wewe.[a]
11 Lakini wote
wanaokukimbilia
watashangilia;[b]
Watapiga vigelegele vya
shangwe[c] mpaka wakati
usio na kipimo.
Nawe utaweka kizuizi
wasifikiwe,
Nao wanaolipenda jina
lako watakushangilia.[d]
12 Kwa maana wewe
mwenyewe utambariki
mtu yeyote aliye
mwadilifu,[e] Ee Yehova;
Kana kwamba kwa ngao[f]
kubwa, utawazunguka
pande zote[g] kwa kibali
chako.

Kwa kiongozi wa vinanda katika sauti ya nane ya chini.[h] Muziki wa Daudi.

6 Ee Yehova, katika hasira
yako usinikaripie,[i]
Na katika ghadhabu yako
usinirekebishe.[j]
2 Nionyeshe kibali, Ee
Yehova, kwa maana
mimi ninafifia.[k]
Niponye,[l] Ee Yehova, kwa
maana mifupa yangu
imesumbuka.
3 Naam, nafsi yangu
imesumbuka sana;[m]
Nawe, Ee Yehova—hata
wakati gani?[n]
4 Urudi,[o] Ee Yehova, uokoe
nafsi yangu;[p]
Uniokoe kwa ajili ya fadhili
zako zenye upendo.[q]
5 Kwa maana katika kifo
wewe hutajwi;[r]

SURA 5

a Zb 89:14; Met 6:16; Hab 1:13; Yak 1:13
b Zb 15:1; Zb 140:13; Met 12:19; Ufu 21:3
c Zb 1:5; 1Ko 1:29
d Met 16:6; Ho 9:15; Mal 2:16; Ro 12:9; Ebr 1:9
e Met 6:19; Met 20:19; Yoh 8:44; Kol 3:9; 1Ti 3:11; Ufu 21:8; Ufu 22:15
f Mwa 4:10; Mwa 9:6; Zb 55:23; Isa 26:21
g Zb 119:163; Met 6:17; Met 12:19; Ho 4:2; 1Pe 3:10
h Zb 51:1; Zb 69:13; Yon 4:2
i 1Sa 3:3; 1Nya 16:1; Zb 84:10
j 1Fa 8:29; Zb 28:2; Zb 138:2
k Zb 23:3; Zb 25:5
l 1Sa 18:14; Zb 27:11; Zb 59:10
m Zb 25:4
n Zb 12:2; Zb 52:2
o Zb 58:2; Mik 6:12
p Zb 140:3; Ro 3:13
q Met 29:5; 1Th 2:5; Yak 3:5
r Ro 3:19
s 2Sa 17:23; Zb 7:15
t 2Sa 15:31; 2Th 1:6

Safu ya 2

a 1Sa 12:15; 1Sa 15:23; Isa 1:20; Isa 63:10; Eze 20:21
b Zb 40:16
c Zb 35:27
d Zb 34:3; Zb 69:36
e Zb 115:13; Met 10:6
f Mwa 15:1; Zb 3:3; Zb 84:11
g Zb 32:10

SURA 6

h 1Nya 15:21; Zb 12:Uta
i Zb 38:1
j Yer 10:24; Yer 46:28
k Zb 38:7; Zb 41:4; 1Pe 1:24; l Zb 103:3; Yer 17:14; Ho 6:1; m Zb 31:9; Mt 26:38; n Zb 13:1; o Zb 90:13; p Zb 17:13; Zb 50:15; q Zb 119:88; Omb 3:22; r Mwa 3:19; Zb 30:9; Zb 88:10; Zb 115:17; Mhu 9:5.

Katika Kaburi* ni nani
atakayekusifu?[a]
6 Nimechoshwa na kuugua
kwangu;[b]
Usiku kucha nafanya
kitanda changu
kilowane;[c]
Kwa machozi yangu
nafanya kitanda
changu kifurike.[d]
7 Kutokana na masumbufu
jicho langu limekuwa
dhaifu,[e]
Limezeeka kwa
sababu ya wale wote
wanaonionyesha uadui.[f]
8 Ondokeni kwangu, ninyi
nyote mnaozoea kutenda
mambo yenye kuumiza,[g]
Kwa maana hakika Yehova
atasikia sauti ya kulia
kwangu.[h]
9 Yehova mwenyewe atasikia
kwelikweli ombi langu la
kutaka kibali;[i]
Yehova ataikubali sala
yangu.[j]
10 Adui zangu wote wataona
aibu[k] sana na kuwa na
wasiwasi;
Watageuka, wataona aibu
ghafula.[l]

Wimbo wa huzuni wa Daudi ambao alimwimbia Yehova kuhusu maneno ya Kushi Mbenyamini.

7 Ee Yehova Mungu wangu,[m]
nimekukimbilia wewe.[n]
Uniokoe kutoka kwa wale
wote wanaonitesa na
unikomboe,[o]
2 Ili mtu yeyote
asiirarue nafsi yangu
vipande-vipande kama
simba anavyofanya,[p]
Kuninyakua wakati
ambapo hakuna
mkombozi.[q]

SURA 6

a Mhu 9:10; Isa 38:18; Yoh 11:13
b Zb 69:3
c 2Sa 13:36; Omb 1:16; Mdo 21:13; 2Ko 2:7
d Zb 39:12
e Ayu 17:7; Zb 31:9
f Zb 88:9
g Zb 119:115; Mt 7:23
h Zb 3:4; Zb 145:18; Isa 30:19; Ebr 5:7
i Zb 31:22; Zb 40:1; Yon 2:2
j Zb 116:1
k Zb 40:14; Zb 109:29; Yer 20:11
l Met 29:1

SURA 7

m Zb 3:7; Zb 35:23
n Zb 18:2; Met 18:10
o Zb 31:15; Yer 15:15; Ro 8:37; 2Ko 4:9; 2Pe 2:9
p Zb 10:9; Zb 17:12; 1Pe 5:8
q Amu 18:28; Zb 50:22

Safu ya 2

a Yos 22:22; 2Sa 16:8
b 1Sa 24:11
c 1Sa 24:17; Met 17:13
d 1Sa 19:4; 1Sa 24:7; 1Sa 26:9
e Mdo 25:11
f Zb 3:7; Zb 68:1; Zb 90:11
g Zb 35:1; Zb 94:2; Isa 33:10
h Zb 44:23; Zb 73:20; Isa 51:9
i Zb 76:9; Zb 103:6
j Mwa 18:25; Zb 9:8
k Zb 18:20; Zb 35:24
l Ayu 27:5; Zb 26:11; Zb 41:12; Zb 78:72; Met 19:1
m Zb 9:5; Met 11:19; Yer 11:20
n Zb 37:25; Met 2:21
o Kum 32:4; 1Nya 28:9; Yoh 17:25; Ufu 15:3
p 1Sa 16:7

3 Ee Yehova Mungu wangu,
ikiwa nimefanya hili,[a]
Ikiwa kuna ukosefu
wowote wa haki katika
mikono yangu,[b]
4 Ikiwa nimemlipa ubaya
yule anayenipa
thawabu,[c]
Au ikiwa nimempora
yeyote anayenionyesha
uadui bila kufanikiwa,[d]
5 Adui na aifuatilie nafsi
yangu[e]
Naye afikie na kukanyagia
chini uhai wangu
Na kufanya utukufu
wangu ukae mavumbini.
Sela.
6 Usimame, Ee Yehova,
katika hasira yako;[f]
Uinuke katika milipuko
ya ghadhabu ya wale
wanaonionyesha uadui,[g]
Na uamke kwa ajili yangu,[h]
kwa maana umetoa amri
kwa ajili ya hukumu.[i]
7 Nalo kusanyiko la vikundi
vya mataifa na
likuzunguke,
Nawe urudi juu dhidi yake.
8 Yehova mwenyewe
atavihukumu vikundi
vya watu.[j]
Nihukumu, Ee Yehova,
kulingana na uadilifu
wangu[k]
Na kulingana na utimilifu[l]
wangu ulio ndani yangu.
9 Tafadhali, ubaya wa waovu
na ufikie mwisho,[m]
Nawe umwimarishe
mwadilifu;[n]
Na Mungu akiwa
mwadilifu[o] anapima
moyo[p] na figo.[q]

Zb 6:5* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

q Yer 11:20; Yer 17:10; Yer 20:12; Ufu 2:23.

10 Ngao yangu iko juu
ya Mungu,[a] Mwokozi wa
wale walio wanyoofu
moyoni.[b]
11 Mungu ni Mwamuzi
mwadilifu,[c]
Na Mungu anazitupa
shutuma kila siku.
12 Ikiwa mtu yeyote
hatarudi,[d] Yeye ataunoa
upanga wake,[e]
Hakika ataupinda upinde
wake, naye atauweka
tayari ili kufyatuliwa.[f]
13 Naye atajitayarishia silaha
za kifo;[g]
Mishale yake ataifanya
kuwa yenye kuwaka
moto.[h]
14 Tazama! Kuna mtu aliye
na mimba ya jambo
lenye kuumiza,[i]
Naye amechukua mimba
ya taabu na hatakosa
kuzaa uwongo.[j]
15 Amechimbua shimo, naye
akalichimba;[k]
Lakini ataanguka katika
shimo alilolifanyiza.[l]
16 Taabu yake itarudi juu
ya kichwa chake
mwenyewe,[m]
Na jeuri yake mwenyewe
itashuka juu ya utosi
wa kichwa chake.[n]
17 Nitamsifu Yehova
kulingana na uadilifu
wake,[o]
Nami nitalipigia muziki
jina[p] la Yehova Aliye
Juu Zaidi.[q]

Kwa kiongozi wa Gitithi.[r]
Muziki wa Daudi.

8 Ee Yehova Bwana wetu,
jina lako ni lenye
utukufu kama nini
katika dunia yote,[s]
Wewe ambaye utukufu
wako unasimuliwa juu
ya mbingu![a]
2 Kutoka katika kinywa cha
watoto na wanaonyonya
umeiweka misingi ya
nguvu,[b]
Kwa sababu ya wale
wanaokuonyesha uadui,[c]
Ili kumkomesha adui
na yule anayejilipizia
kisasi.[d]
3 Ninapoziona mbingu zako,
kazi za vidole vyako,[e]
Mwezi na nyota ambazo
umetayarisha,[f]
4 Mwanadamu anayeweza
kufa[g] ni nini hivi
kwamba umweke
akilini,[h]
Na mwana wa mtu
wa udongo hivi kwamba
umtunze?[i]
5 Pia ulimfanya mdogo
kidogo kuliko wale walio
kama Mungu,[j]
Kisha ulimvika taji[k] la
utukufu[l] na fahari.
6 Unamfanya atawale juu ya
kazi za mikono yako;[m]
Kila kitu umekiweka chini
ya miguu yake:[n]
7 Kondoo na mbuzi na
ng'ombe, wote hao,[o]
Na pia wanyama wa
porini,[p]
8 Ndege wa mbinguni na
samaki wa baharini,[q]
Kitu chochote kinachopita
katika njia za baharini.[r]
9 Ee Yehova Bwana wetu,
jina lako ni lenye
utukufu kama nini
katika dunia yote![s]

SURA 7

a Mwa 15:1; Met 30:5
b Zb 125:4; Met 2:21
c Mwa 18:25; Zb 9:4; Zb 33:5; Zb 98:9
d Zb 85:4; Isa 55:7; Mal 4:6; Lu 1:16
e Kum 32:41; Eze 21:9
f Kum 32:23
g Hab 3:5
h Kum 32:42; Zb 45:5; Zb 64:7
i Isa 33:11
j Isa 59:4; Yak 1:15
k Zb 35:7; Zb 40:2; Zb 57:6; Yer 18:20
l Est 7:10; Zb 10:2; Met 26:27
m 1Fa 2:32; Est 9:25; Ga 6:7
n Mt 26:52
o Zb 35:28; Zb 51:14; Zb 71:15; Zb 98:2; Zb 145:7
p Zb 9:2; Isa 25:1; Ebr 13:15
q Mwa 14:22; Zb 83:18; Zb 92:8; Da 4:17; Ufu 15:4

SURA 8

r Zb 84:Uta
s Kum 28:58; Zb 148:13; Mt 6:9; Yoh 17:26

Safu ya 2

a 1Fa 8:27; 1Nya 16:27; Ayu 37:22; Zb 104:1; Zb 148:13; Isa 33:21; Ebr 1:3
b Mt 21:16; Lu 10:21; Mdo 4:13; 1Ko 1:27
c Mdo 4:14; Mdo 6:10
d Zb 44:16
e Mwa 1:1; Zb 19:1; Zb 102:25; Ro 1:20
f Zb 104:19; Isa 40:26; Mt 5:45
g Isa 51:12; 1Ko 15:47
h Ayu 7:17; Zb 144:3; Ebr 2:6

i Mwa 1:29; Mwa 9:3; Mt 6:25; Mt 6:30; Lu 12:28; Yoh 3:16; Mdo 14:17; j Ebr 2:7; k Isa 40:5; 1Ko 11:7; l Zb 21:5; Met 5:9; m Mwa 1:26; Mwa 9:2; n Ebr 2:8; o Mwa 1:28; Mwa 9:3; p Mwa 2:20; q Mwa 1:20; Yoh 21:6; r Mwa 1:21; Ayu 41:1; s Zb 8:1; Ebr 8:1.

Kwa kiongozi wa Muth-labeni.
Muziki wa Daudi.

א [*'A'leph*]

9 Nitakusifu wewe, Ee
Yehova, kwa moyo
wangu wote;[a]
Nitazitangaza kazi zako
zote za ajabu.[b]
2 Nitakushangilia na
kukufurahia,[c]
Nitalipigia jina lako
muziki, Ee Uliye
Juu Zaidi.[d]

ב [*Behth*]

3 Adui zangu wanapogeuka
nyuma,[e]
Watajikwaa na kuangamia
kutoka mbele zako.[f]
4 Kwa maana umetekeleza
hukumu yangu na kesi
yangu;[g]
Umeketi juu ya kiti cha
ufalme ukihukumu
kwa uadilifu.[h]

ג [*Gi'mel*]

5 Umeyakemea mataifa,[i]
umemwangamiza
mwovu.[j]
Jina lao umelifutilia mbali
mpaka wakati usio na
kipimo, naam, milele.[k]
6 Ewe adui, ukiwa wako
umefikia mwisho wake
wa kudumu,[l]
Na majiji ambayo
umeyang'oa.[m]
Kumbukumbu lao hakika
litaangamia.[n]

ד [*He'*]

7 Yeye Yehova ataketi mpaka
wakati usio na kipimo,[o]
Akifanya imara kiti chake
cha ufalme kwa ajili ya
hukumu.[p]
8 Naye mwenyewe
ataihukumu kwa uadilifu
nchi yenye kuzaa;[q]

SURA 9

a Zb 86:12
Zb 111:1
b 1Nya 16:12
1Nya 29:11
Ufu 4:11
c Zb 5:11
Zb 28:7
d Zb 83:18
Zb 97:9
Ufu 15:3
e Zb 56:9
f Zb 80:16
g Zb 140:12
h Zb 89:14
Zb 98:9
1Pe 2:23
i Kum 9:4
j Zb 106:11
k Kum 9:14
Mt 25:46
l Kut 14:13
Zb 34:16
m 1Sa 31:7
n Kum 25:19
Isa 14:22
o Zb 90:2
Zb 102:12
1Ti 1:17
p Zb 89:14
Ro 14:10
Ufu 20:11
q Mwa 18:25
Zb 85:11
Zb 96:13
Isa 26:9

Safu ya 2

a Zb 98:9
Mdo 17:31
b Zb 32:7
Zb 46:1
Zb 91:2
Ufu 7:10
c Zb 54:7
d Zb 91:14
Met 18:10
Yer 16:21
e 2Nya 20:12
Zb 25:15
2Ko 1:10
f Zb 74:2
Zb 132:13
Zb 135:21
g Zb 66:5
Zb 96:10
Zb 105:1
Zb 107:22
Isa 12:4
h Mwa 4:10
2Fa 9:26
i Mwa 9:5
Kum 32:43
2Fa 24:4
Isa 26:21
Lu 11:50
j Kut 3:7
Zb 72:14
Lu 18:7
k Zb 25:19
l 2Sa 22:5
Ayu 38:17
Zb 30:3
Zb 107:18
Zb 116:3
Isa 38:10
Ufu 1:18
m Zb 66:16
n Yer 17:19
o Isa 37:22
p Zb 13:5
Zb 20:5
Hab 3:18
q Zb 7:15

Atavihukumu vikundi vya
mataifa kwa unyoofu.[a]

ו [*Waw*]

9 Naye Yehova
atakuwa kilele salama
kwa ajili ya mtu yeyote
aliyekandamizwa,[b]
Kilele salama wakati
wa taabu.[c]
10 Na wale wanaolijua jina
lako watakutegemea,[d]
Kwa maana hakika
hutawaacha wale
wanaokutafuta,
Ee Yehova.[e]

ז [*Za'yin*]

11 Mpigieni Yehova muziki,
yeye anayekaa Sayuni;[f]
Tangazeni matendo yake
katikati ya vikundi vya
watu.[g]
12 Kwa maana, wakati
wa kutafuta umwagikaji
wa damu,[h] hakika
atawakumbuka hao;[i]
Hakika yeye hatakisahau
kilio cha wenye
kuteseka.[j]

ח [*Chehth*]

13 Unionyeshe kibali, Ee
Yehova; uone mateso
yangu kutoka kwa wale
wanaonichukia,[k]
Ewe unayeniinua kutoka
katika malango ya kifo,[l]
14 Ili niyatangaze matendo
yako yote yanayostahili
sifa[m]
Katika malango[n] ya binti
Sayuni,[o]
Ili niushangilie wokovu
wako.[p]

ט [*Tehth*]

15 Mataifa yamezama katika
shimo walilolifanya;[q]

Mguu wao wenyewe
umekamatwa[a] katika
wavu[b] walioficha.
16 Yehova anajulikana
kwa hukumu ambayo
ametekeleza.[c]
Mwovu amenaswa na
utendaji wa mikono yake
mwenyewe.[d]
Higayoni. *Sela*.

[*Yohdh*]

17 Watu waovu[e] watarudi
katika Kaburi,*[f]
Naam, mataifa yote
yanayomsahau Mungu.[g]
18 Kwa maana maskini
hawatasahauliwa
sikuzote,[h]
Wala tumaini la wapole
halitaangamia kamwe.[i]

[*Kaph*]

19 Usimame, Ee Yehova!
Mwanadamu anayeweza
kufa asiwe na nguvu
zaidi.[j]
Mataifa na yahukumiwe
mbele za uso wako.[k]
20 Utie woga ndani yao, Ee
Yehova,[l]
Ili mataifa yapate kujua
kwamba wao ni
wanadamu tu
wanaoweza kufa.[m] *Sela*.

[*La′medh*]

10 Ee Yehova, kwa nini
unaendelea kusimama
mbali?[n]
Kwa nini unaendelea
kujificha nyakati
za taabu?[o]
2 Katika majivuno yake,
mwovu humfuatilia
vikali mwenye
kuteseka;[p]
Wanakamatwa na mawazo
ambayo wametunga.[q]
3 Kwa maana mwovu
amejisifu kwa sababu ya
tamaa yenye ubinafsi ya
nafsi yake,[a]
Naye anayepata faida
asiyostahili[b] amejibariki;

[*Nun*]

Amekosa kumheshimu
Yehova.[c]
4 Kwa sababu ya kujigamba
kwake, mwovu hatafuti;[d]
Mawazo yake yote ni:
“Hakuna Mungu.”[e]
5 Njia zake zinaendelea
kufanikiwa wakati wote.[f]
Maamuzi yako ya hukumu
yako juu sana asiweze
kuyafikia;[g]
Nao wale wote
wanaomwonyesha uadui,
anawafanyia dhihaka.[h]
6 Amesema katika moyo
wake: “Sitatikiswa;[i]
Kizazi baada ya kizazi
sitakuwa katika msiba.”[j]

[*Pe′*]

7 Kinywa chake kimejaa
viapo na udanganyifu
na ukandamizaji.[k]
Chini ya ulimi wake kuna
taabu na mambo yenye
kuumiza.[l]
8 Yeye huketi akivizia
makao;
Kutoka mafichoni atamuua
mtu asiye na hatia.[m]

[*′A′yin*]

Macho yake yanamtafuta
mtu mwenye taabu.[n]
9 Yeye anaendelea
kuvizia katika mahali
palipofichika kama
simba mafichoni mwake.[o]

Zb 9:17* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

SURA 9

a Kum 32:35 Zb 35:8 Met 5:22
b Zb 35:7 Zb 57:6 Zb 141:10
c Kut 14:4 Yos 2:10 1Sa 6:20 2Fa 19:19
d Met 6:2 Met 26:27 Isa 3:11
e Zb 49:14
f Hes 16:30 Isa 5:14
g Zb 50:22 Isa 34:2 Yer 10:25
h Zb 12:5 Zb 72:4
i Zb 10:17 Zb 37:34 Met 24:14 Mt 5:5
j 1Sa 2:9 Da 5:21
k Mwa 18:25 Zb 82:8 Mdo 17:31
l Kut 15:16 Kut 23:27 Kum 2:25
m Ayu 40:12 Isa 31:3 Eze 28:2 Mdo 12:23

SURA 10

n Zb 22:1 Yer 14:8
o Zb 13:1 Zb 44:24
p Kut 14:17 Zb 37:14
q Mwa 11:4 Zb 7:16 Zb 21:11 Zb 37:7 Met 5:22 Met 26:27 Ufu 17:13

Safu ya 2

a Kut 15:9 Zb 94:4 Zb 106:14 Ho 12:8
b Met 11:18 Yak 5:4
c Isa 57:17 Mk 12:9 Lu 20:15
d Ayu 35:10 Zb 14:2 Yer 2:6
e Zb 14:1 Zb 53:1 Sef 1:12
f Zb 37:35
g Met 24:1 Isa 26:11 Ho 14:9
h Zb 12:5
i Met 14:16
j Mhu 8:11 Isa 56:12 Ufu 18:7
k Zb 5:6 Zb 59:12 Ro 3:14 1Pe 3:10
l Zb 7:14; Zb 12:2; Zb 55:21; Met 10:31; Met 17:4; **m** Met 1:11; Hab 3:14; **n** Zb 17:11; Yer 22:17; **o** Zb 17:12; Zb 59:3; Mik 7:2; Mdo 23:21.

Anaendelea kuvizia[a] ili
amchukue kwa nguvu
mtu fulani mwenye
kuteseka.
Humchukua kwa nguvu
mtu mwenye kuteseka
anapouvuta pamoja
wavu wake.[b]
10 Yeye anapondwa,
anainama,
Na jeshi la watu
waliohuzunika
linaangukia kucha
zake zenye nguvu.[c]
11 Yeye amesema katika
moyo wake:[d] "Mungu
amesahau.[e]
Ameuficha uso wake.[f]
Hakika hatauona kamwe."[g]

ק [*Qohph*]

12 Usimame,[h] Ee Yehova. Ee
Mungu, uinue mkono
wako.[i]
Usiwasahau wenye
kuteseka.[j]
13 Kwa nini mwovu amekosa
kumheshimu Mungu?[k]
Amesema katika moyo
wake: "Wewe hutatoza
hesabu."[l]

ר [*Rehsh*]

14 Kwa maana wewe
mwenyewe umeona
taabu na masumbufu.
Unaendelea kutazama,
uyatie katika mkono
wako.[m]
Mtu mwenye taabu,[n]
mvulana asiye na baba,
anajikabidhi kwako.
Wewe mwenyewe
umekuwa msaidizi
wake.[o]

ש [*Shin*]

15 Uvunje mkono wa mwovu
na mbaya.[p]
Uutafute uovu wake
mpaka usiupate tena.[q]

SURA 10

a Ayu 38:40
Omb 3:10
b Ayu 18:8
Zb 140:5
Yer 5:26
Hab 1:15
Yoh 10:12
c 2Sa 15:5
d Zb 10:6
Mk 2:6
e Zb 64:5
Mhu 8:11
f Zb 51:9
Zb 73:11
g Zb 94:7
Eze 8:12
Eze 9:9
h Zb 3:7
i Zb 94:2
Mik 5:9
j Zb 9:12
Zb 35:10
k Kum 31:20
Zb 74:10
l Ebr 4:13
m 2Fa 9:26
2Nya 6:23
n 2Ti 1:12
1Pe 4:19
o Kum 10:18
Zb 146:9
Yer 49:11
Ho 14:3
Ebr 13:6
p Ayu 34:30
Ayu 38:15
Zb 37:17
Eze 30:21
Zek 11:17
q 2Fa 21:13
Zb 4:5
1Th 5:22

Safu ya 2

a Zb 29:10
Zb 145:13
Yer 10:10
Da 4:34
1Ti 1:17
b Zb 9:5
Zb 44:2
c Zb 9:18
Zb 147:6
d 1Nya 29:18
2Nya 30:12
e 1Sa 8:21
Zb 6:9
Zb 9:18
Zb 102:17
Met 15:8
1Pe 3:12
1Yo 3:22
f Zb 72:4
Zb 82:3
g Isa 51:12

SURA 11

h 2Nya 14:11
Zb 7:1
Zb 56:11
i Met 27:8
j Zb 37:14
k Mdo 23:15
l Zb 82:5
m Isa 6:1
Mik 1:2
Hab 2:20
Ufu 7:15
n 2Nya 20:6
Zb 103:19
Mt 23:22
Mdo 7:49
Ufu 4:2

16 Yehova ni Mfalme mpaka
wakati usio na kipimo,
naam, milele.[a]
Mataifa yameangamia
kutoka katika dunia
yake.[b]

ת [*Taw*]

17 Tamaa ya wapole hakika
utaisikia,[c] Ee Yehova.
Utautayarisha moyo wao.[d]
Utasikiliza kwa makini
kwa sikio lako.[e]
18 Ili kumhukumu mvulana
asiye na baba na mtu
aliyependwa,[f]
Ili mwanadamu anayeweza
kufa, aliye wa dunia,
asisababishe tena
kutetemeka.[g]

Kwa kiongozi. Ya Daudi.

11 Nimemkimbilia Yehova.[h]
Mnawezaje kuthubutu
kuiambia nafsi yangu:
"Kimbieni kwenye mlima
wenu kama ndege![i]
2 Kwa maana, tazama!
waovu huupinda upinde,[j]
Huutayarisha mshale wao
juu ya kamba ya upinde,
Ili katika giza wawafyatulie
walio wanyoofu moyoni.[k]
3 Misingi inapobomolewa,
Yeyote aliye mwadilifu
afanye nini?"[l]
4 Yehova yumo katika
hekalu lake takatifu.[m]
Yehova—kiti chake cha
ufalme kiko mbinguni.[n]
Macho yake yanaangalia,
macho yake yanayong'aa
yanawachunguza[o] wana
wa binadamu.
5 Yehova humchunguza
mwadilifu na pia
mwovu,[p]

o 2Nya 16:9; Zb 33:13; Zb 66:7; Met 15:3; Zek 4:10; Ebr 4:13; p Mwa 6:5; Mwa 7:1; Mwa 22:1.

Na mtu yeyote anayependa
jeuri nafsi Yake hakika
inamchukia.[a]
6 Yeye atawanyeshea waovu
mitego, moto na kiberiti[b]
Na upepo wenye kuunguza,
vikiwa fungu la kikombe
chao.[c]
7 Kwa maana Yehova ni
mwadilifu;[d] yeye
huyapenda matendo
ya uadilifu.[e]
Wanyoofu ndio
watakaouona uso wake.[f]

Kwa kiongozi katika sauti ya nane ya chini.[g] Muziki wa Daudi.

12 Uniokoe,[h] Ee Yehova,
kwa maana
mshikamanifu
amefikia mwisho;[i]
Kwa maana watu
waaminifu wametoweka
kutoka katikati ya wana
wa binadamu.
2 Wao huendelea
kusemezana mambo
yasiyo ya kweli;[j]
Kwa midomo laini[k] wao
huendelea kusema
wakiwa na mioyo miwili.[l]
3 Yehova ataikata midomo
yote iliyo laini,
Ulimi unaosema maneno
makuu,[m]
4 Wale ambao wamesema:
"Kwa ulimi wetu
tutashinda.[n]
Midomo yetu iko
pamoja nasi. Ni nani
atakayekuwa bwana
kwetu?"
5 "Kwa sababu ya kuporwa
kwao wenye kuteseka,
kwa sababu ya kuugua
kwao maskini,[o]
Nitasimama wakati huu,"
asema Yehova.[p]
"Nitamweka katika
usalama mbali na mtu
yeyote anayemdhihaki."[a]
6 Maneno ya Yehova ni
maneno safi,[b]
Kama fedha iliyosafishwa
katika tanuru ya
kuyeyushia kwenye
udongo, iliyosafishwa
mara saba.
7 Wewe mwenyewe, Ee
Yehova, utawalinda;[c]
Utamhifadhi kila mmoja
kutokana na kizazi hiki
mpaka wakati usio na
kipimo.
8 Waovu wanatembea
kuzunguka pande zote,
Kwa sababu uovu
unatukuzwa katikati ya
wana wa binadamu.[d]

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

13 Utanisahau mpaka
wakati gani, Ee
Yehova?[e] Milele?[f]
Utanificha uso wako
mpaka wakati gani?[g]
2 Nitaweka upinzani katika
nafsi yangu mpaka
wakati gani,
Huzuni katika moyo
wangu wakati wa
mchana?
Adui yangu atainuliwa juu
yangu mpaka wakati
gani?[h]
3 Unitazame; unijibu, Ee
Yehova Mungu wangu.
Uyafanye macho yangu
yang'ae,[i] ili nisilale
usingizi katika kifo.[j]
4 Ili adui yangu asiseme:
"Nimemshinda!"
Ili wapinzani wangu
wasishangilie kwa
sababu nimefanywa
niyumbe-yumbe.[k]

SURA 11
a Met 3:31; Met 6:17
b Mwa 19:24; Eze 38:22
c Zb 75:8; Isa 51:17; Yer 25:15; Hab 2:16; Ufu 16:19; Ufu 18:6
d Kum 32:4
e Zb 45:7; Zb 146:8
f Ayu 36:7; Zb 34:15; 1Pe 3:12

SURA 12
g Zb 6:Uta
h Zb 3:7
i Mik 7:2
j Zb 10:7; Zb 41:6
k Zb 5:9; Zb 28:3; Zb 62:4; Yer 9:8; Ro 16:18
l 1Nya 12:33
m Kut 15:9; 1Sa 2:3; Zb 17:10; Eze 28:2; 2Pe 2:18
n Yer 18:18
o Kut 3:7; Zb 10:12
p Isa 33:10

Safu ya 2
a Zb 10:5
b 2Sa 22:31; Zb 18:30; Zb 19:8; Zb 119:140; Met 30:5
c 1Sa 2:9; Zb 145:20
d Mhu 8:11

SURA 13
e Zb 6:3; Zb 88:14; Isa 59:2
f Omb 5:20
g Kum 31:17; Ayu 13:24; Zb 22:2; Isa 59:2
h Zb 22:7
i Ezr 9:8
j Yer 51:39; Yoh 11:11
k Zb 25:2; Zb 35:19; Zb 38:16; Omb 1:16

5 Nami nimezitegemea
fadhili zako zenye
upendo;[a]
Moyo wangu na ushangilie
katika wokovu wako.[b]
6 Nitamwimbia Yehova, kwa
maana amenitendea kwa
njia ya kunipa thawabu.[c]

Kwa kiongozi. Ya Daudi.

14 Asiye na akili amesema
katika moyo wake:
"Hakuna Yehova."[d]
Wametenda kwa
uharibifu,[e] wametenda
kwa njia yenye
kuchukiza katika
shughuli zao.
Hakuna yeyote
anayefanya mema.[f]
2 Kutoka mbinguni Yehova
amewatazama wana wa
binadamu walio chini,[g]
Ili aone kama kuna yeyote
ambaye ana ufahamu,
yeyote anayemtafuta
Yehova.[h]
3 Wote wamegeuka kando,[i]
wote ni wafisadi kwa
njia ileile;[j]
Hakuna yeyote
anayefanya mema,[k]
Hakuna hata mmoja.[l]
4 Je, hakuna yeyote kati ya
wale wanaotenda mambo
yenye kuumiza ambaye
ana ujuzi,[m]
Wakila watu wangu kama
vile ambavyo wamekula
mkate?[n]
Hata hawajamwitia
Yehova.[o]
5 Hapo wao walijawa na
hofu kubwa,[p]
Kwa maana Yehova yuko
kati ya kizazi cha
mwadilifu.[q]

SURA 13

a Zb 52:8
Zb 147:11
1Pe 5:7
b 1Sa 2:1
Lu 1:47
c Zb 116:7
Zb 119:17

SURA 14

d Zb 10:4
Zb 53:1
Isa 29:16
e Mwa 6:12
f Ro 3:10
g Mwa 11:5
Zb 33:13
Zb 102:19
h 2Nya 16:9
Ebr 11:6
i Mhu 7:29
j Isa 64:6
k Ro 3:11
l Ro 3:10
m Zb 94:8
n Yer 10:25
Amo 8:4
Mik 3:3
o Zb 79:6
Isa 64:7
p Kut 15:16
Zb 53:5
q Zb 24:6

Safu ya 2

a Zb 9:9
Zb 142:5
Ebr 6:18
b Ro 11:26
c Zb 53:6
Zb 85:1
Zb 126:4
d Ne 12:43
Zb 126:1

SURA 15

e Ufu 21:3
f Zb 2:6
Zb 3:4
Zb 24:3
Isa 2:3
g Zb 1:1
h Zb 50:23
Isa 33:15
Mdo 10:35
i Met 3:32
Met 12:19
Zek 8:16
Efe 4:25
Kol 3:9
j Law 19:16
Zb 34:13
Zb 101:5
Met 11:13
Met 20:19
Met 30:10
k 1Sa 24:11
Met 14:21
Ro 12:17
l Kut 23:1
m Est 3:2
n Zb 101:6
o Yos 9:18
Amu 11:35
Zb 50:14
Mt 5:33
p Kut 22:25
Law 25:36
Kum 23:19
Eze 18:17
q Kut 23:8
Kum 16:19

6 Shauri la mwenye
kuteseka ninyi
huliaibisha,
Kwa sababu Yehova ni
kimbilio lake.[a]
7 Laiti wokovu wa Israeli
ungetoka Sayuni![b]
Wakati ambapo Yehova
anawakusanya tena
mateka wa watu wake,[c]
Yakobo na ashangilie,
Israeli na afurahi.[d]

Muziki wa Daudi.

15 Ee Yehova, ni nani
atakayekuwa mgeni
katika hema lako?[e]
Ni nani atakayekaa katika
mlima wako mtakatifu?[f]
2 Yeye anayetembea bila
kosa[g] na kuzoea
kutenda uadilifu[h]
Na kusema kweli katika
moyo wake.[i]
3 Yeye hakuchongea kwa
ulimi wake.[j]
Hakumfanyia mwenzake
jambo lolote baya,[k]
Wala hakumshutumu
rafiki yake.[l]
4 Machoni pake mtu yeyote
mwenye kudharaulika
hakika amekataliwa,[m]
Lakini yeye
anawaheshimu wale
wanaomwogopa Yehova.[n]
Ameapa juu ya jambo lililo
baya kwake, na bado
yeye habadiliki.[o]
5 Pesa zake hakutoa ili apate
faida,[p]
Wala hakuchukua rushwa
dhidi ya mtu asiye na
hatia.[q]
Yeye anayefanya mambo
hayo hatatikiswa.[r]

r Zb 16:8; Zb 55:22; Met 12:3; 2Pe 1:10.

Miktamu ya Daudi.

16 Unihifadhi, Ee
Mungu, kwa maana
nimekukimbilia
wewe.[a]
2 Nimemwambia Yehova:
"Wewe ni Yehova; wema
wangu si kwa ajili yako,[b]
3 Bali kwa watakatifu walio
duniani.
Wao, naam, wale
mashuhuri, ndio
ninaopendezwa nao
kabisa."[c]
4 Maumivu huwa mengi kwa
wale ambao, wakati kuna
mtu mwingine, humfuata
haraka.[d]
Sitamimina matoleo yao ya
kinywaji ya damu,[e]
Nami sitayachukua majina
yao juu ya midomo
yangu.[f]
5 Yehova ndiye sehemu
ya fungu langu[g]
nililogawiwa na ya
kikombe changu.[h]
Wewe unaishika sana kura
yangu.
6 Kamba za kupimia
zimeniangukia mahali
panapopendeza.[i]
Kwa kweli, miliki yangu
mwenyewe naikubali.
7 Nitambariki Yehova,
ambaye amenipa shauri.[j]
Kwa kweli, nyakati
za usiku figo zangu
zimenirekebisha.[k]
8 Nimemweka Yehova mbele
yangu daima.[l]
Kwa sababu yuko upande
wa mkono wangu wa
kuume, sitatikiswa.[m]
9 Kwa hiyo moyo
wangu unashangilia, nao
utukufu wangu una
mwelekeo wa kuwa na
shangwe.[n]

SURA 16

a Zb 25:20
Zb 91:2
b Ayu 35:7
Ro 11:35
c Zb 119:63
d Kum 8:19
Zb 97:7
Yon 2:8
e Yer 7:18
f Kut 23:13
Yos 23:7
Ho 2:17
g Hes 18:20
Zb 73:26
Omb 3:24
h Zb 23:5
i Zb 78:55
j Isa 48:17
k Zb 17:3
Zb 26:2
l Zb 139:18
Mdo 2:25
m Zb 73:23
Zb 121:5
n Zb 30:12
Zb 57:8

Safu ya 2

a Ayu 14:14
Isa 26:19
b Zb 49:15
Met 15:11
Mdo 2:31
Mdo 3:15
Ufu 1:18
c Ayu 14:13
Ayu 17:14
Isa 38:17
Mdo 13:35
d Zb 21:4
Met 12:28
e Zb 21:6
Mt 5:8
Mdo 2:28
1Ti 1:11
f Zb 36:10

SURA 17

g Zb 5:2
h Zb 145:18
i Zb 37:6
j Ayu 1:8
k Zb 11:5
Zb 16:7
1Ko 4:4
l Ayu 23:10
Zb 26:2
Zb 66:10
Yer 9:7
Zek 13:9
Mal 3:3
1Pe 1:7
m Zb 39:1
n Zb 119:9
o 1Sa 2:9
Zb 119:133
p Zb 18:36
Zb 94:18
Zb 121:3

Pia, mwili wangu
mwenyewe utakaa
katika usalama.[a]
10 Kwa maana hutaiacha
nafsi yangu katika
Kaburi.*[b]
Hutamruhusu
mshikamanifu wako
aone shimo.[c]
11 Utanijulisha njia ya uzima.[d]
Shangwe ya kutosha iko
pamoja na uso wako;[e]
Kuna uzuri upande wa
mkono wako wa kuume
milele.[f]

Sala ya Daudi.

17 Usikie jambo la uadilifu,
Ee Yehova; Usikilize
kwa makini kilio
changu cha kusihi;[g]
Tega sikio kwa sala
yangu bila midomo ya
udanganyifu.[h]
2 Hukumu yangu na itoke
mbele zako;[i]
Macho yako mwenyewe na
yaone unyoofu.[j]
3 Umeuchunguza moyo
wangu, umefanya
ukaguzi wakati wa
usiku,[k]
Umenisafisha; utagundua
kwamba sijapanga hila.[l]
Kinywa changu
hakitafanya kosa.[m]
4 Nao utendaji wa
wanadamu,
Kwa maneno ya midomo
yako mimi mwenyewe
nimejilinda na njia za
mnyang'anyi.[n]
5 Hatua zangu na zishike
njia zako,[o]
Ambamo hatua za
miguu yangu hakika
hazitatikiswa.[p]

Zb 16:10* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

6 Mimi mwenyewe nakuitia
wewe, kwa sababu
utanijibu, Ee Mungu.[a]
Tega sikio lako kwangu.
Usikilize neno langu.[b]
7 Uyafanye matendo yako
ya fadhili zenye upendo
yawe ya ajabu,[c] Ee
Mwokozi wa wale
wanaotafuta kimbilio
Kutoka kwa waasi walio
dhidi ya mkono wako wa
kuume.[d]
8 Unitunze kama mboni ya
jicho,[e]
Katika kivuli cha mabawa
yako unifiche,[f]
9 Kwa sababu ya waovu
ambao wamenipora.
Adui za nafsi yangu
wanazidi kunizingira.[g]
10 Wamejizungushia mafuta
yao wenyewe;[h]
Kwa vinywa vyao
wamesema kwa
majivuno;[i]
11 Sasa wametuzingira hatua
zetu;[j]
Wanakaza macho yao ili
kuelekeza duniani.[k]
12 Mfano wake ni ule
wa simba anayetamani
kurarua
vipande-vipande[l]
Na ule wa mwana-simba
anayekaa mahali
palipofichika.
13 Usimame, Ee Yehova;
umkabili usoni;[m]
Mfanye ainame; kwa
upanga wako uiokoe
nafsi yangu kutoka
kwa mwovu,[n]
14 Kwa mkono wako, Ee
Yehova, kutoka kwa
watu,[o]
Kutoka kwa watu wa
mfumo huu wa mambo,[a]
ambao fungu lao liko
katika maisha haya,[b]
Na ambao tumbo lao wewe
hulijaza kwa hazina
iliyofichwa,[c]
Ambao wametosheka na
wana[d]
Na ambao huwarundikia
watoto wao vitu
wanavyoacha.[e]
15 Nami, katika uadilifu
nitauona uso wako;[f]
Nitatosheka kuliona umbo
lako ninapoamka.[g]

Kwa kiongozi. Wa mtumishi wa Yehova, wa Daudi, aliyemwambia Yehova maneno ya wimbo huu siku ambayo Yehova alikuwa amemkomboa kutoka mkononi mwa adui zake wote na kutoka mkononi mwa Sauli.[h] Naye akasema:

18 Nitakupenda wewe,
Ee Yehova nguvu
zangu.[i]
2 Yehova ni mwamba wangu
na ngome yangu na
Mwokoaji wangu.[j]
Mungu wangu ni mwamba
wangu. Nitamkimbilia,[k]
Ngao yangu na pembe
yangu ya wokovu, kilele
changu salama.[l]
3 Nitamwita, Yehova, Yule
anayestahili kusifiwa,[m]
Nami nitaokolewa kutoka
kwa adui zangu.[n]
4 Kamba za kifo
zilinizunguka;[o]
Mafuriko ya ghafula ya
watu wasiofaa kitu pia
yaliendelea
kuniogopesha.[p]
5 Kamba za Kaburi*
zilinizunguka;[q]
Mitego ya kifo ilinikabili.[r]

SURA 17
a Zb 55:16; Zb 66:19
b Zb 116:2; Isa 37:17
c Zb 31:21; Omb 3:22
d Kut 15:6
e Kum 32:10; Zek 2:8
f Ru 2:12; Zb 36:7; Zb 57:1; Zb 63:7
g 1Sa 24:11; Zb 35:4
h Kum 32:15; Zb 119:70; Eze 16:49
i 1Sa 2:3; Zb 31:18; Zb 73:9
j 1Sa 23:26
k Zb 10:8
l Zb 7:2
m Zb 7:6
n Zb 7:12
o Zb 108:6

Safu ya 2
a Zb 49:1; 1Ti 6:17
b Zb 73:12; Yak 5:5
c Ayu 22:18; Zb 144:13; Mt 5:45
d Zb 144:12
e Zb 39:6
f Ayu 19:26
g Zb 65:4

SURA 18
h 2Sa 22:1
i Zb 18:32; Zb 118:14; Isa 12:2
j Zb 3:3; Zb 37:40; Zb 40:17; Zb 70:5; Zb 144:2
k 2Sa 23:3; Zb 46:1
l Mwa 15:1; Kum 32:4; 2Sa 22:3; Met 2:7; Lu 1:69
m 2Sa 22:4; Zb 69:34; 2Ko 11:31
n Zb 50:15; Lu 1:71
o 1Sa 20:3; Zb 116:3; Mt 26:66
p 2Sa 20:1; 2Sa 22:5; Zb 22:16
q 2Sa 22:6; Zb 88:3
r Mhu 9:12

Zb 18:5* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

6 Katika taabu yangu
niliendelea kumwita
Yehova,
Nami niliendelea kumlilia
Mungu wangu kwa ajili
ya msaada.[a]
Kutoka katika hekalu lake
aliisikia sauti yangu,[b]
Nacho kilio changu
cha msaada mbele zake
sasa kikafika masikioni
mwake.[c]
7 Na dunia ikaanza
kutikisika na
kutetemeka,[d]
Nayo misingi ya milima
ikasukasuka,[e]
Nayo ikatikisika huku
na huku kwa sababu
alikuwa amekasirishwa.[f]
8 Moshi ukapanda katika
mianzi ya pua yake, nao
moto kutoka kinywani
mwake ukaendelea
kuteketeza;[g]
Makaa yakawaka moto
kutoka kwake.
9 Naye akaziinamisha
mbingu, akashuka.[h]
Na giza zito lilikuwa chini
ya miguu yake.
10 Naye akaja akiwa
amepanda juu ya kerubi,
akaja akiwa anaruka,[i]
Naye akaja akiruka juu
ya mabawa ya roho.[j]
11 Kisha akalifanya giza
kuwa mahali pake pa
kujificha,[k]
Kama kibanda cha
kumzunguka pande zote,
Maji yenye giza, mawingu
mazito.[l]
12 Kutoka katika mwangaza
ulio mbele yake
kulikuwa na mawingu
yake yaliyopita,[m]
Mvua ya mawe na makaa
yanayowaka moto.[n]

SURA 18

a Zb 50:15
Zb 130:1
b 1Sa 3:3
2Sa 22:7
1Nya 16:1
Zb 11:4
Yon 2:7
c Kut 3:7
Zb 10:17
Zb 34:15
1Pe 3:12
d Amu 5:4
Eze 38:19
Hag 2:6
e 2Sa 22:8
f Zb 77:18
Zb 97:4
Ufu 16:18
g 2Sa 22:9
Isa 30:27
h 2Sa 22:10
Zb 144:5
Isa 64:1
i Zb 99:1
j Zb 104:3
Ebr 1:7
k Zb 97:2
l Ayu 36:29
m 2Sa 22:13
n Zb 97:3

Safu ya 2

a 1Sa 2:10
1Sa 7:10
b 2Sa 22:14
Zb 29:3
c Yos 10:10
Isa 30:30
d 2Sa 22:15
Ayu 36:32
Zb 144:6
e Zb 74:15
Zb 106:9
Zb 114:3
f 2Sa 22:16
Zb 9:8
g Kut 15:8
h 2Sa 22:17
Zb 57:3
i Zb 32:6
Zb 124:4
j 2Sa 22:18
Zb 3:7
k Zb 35:10
l 1Sa 19:11
1Sa 23:26
m Isa 50:10
n Zb 31:8
Zb 118:5
o Zb 149:4
p 1Sa 26:23
1Fa 8:32
Met 11:18
q 1Sa 24:11
Zb 24:4
r 2Sa 22:22

13 Na mbinguni Yehova
akaanza kunguruma,[a]
Na Aliye Juu Zaidi akaanza
kutoa sauti yake,[b]
Mvua ya mawe na makaa
yanayowaka moto.
14 Naye akaendelea kuitupa
mishale yake, ili
awatawanye;[c]
Naye akatupa umeme, ili
awavuruge.[d]
15 Na sakafu za vijito vya
maji zikaonekana,[e]
Na misingi ya nchi yenye
kuzaa ikafunuliwa,[f]
Kwa kemeo lako, Ee
Yehova, kwa mlipuko
wa pumzi ya pua yako.[g]
16 Alikuwa akituma mkono
kutoka juu, alikuwa
akinichukua,[h]
Alikuwa akinitoa ndani
ya maji makuu.[i]
17 Alikuwa akinikomboa
kutoka kwa adui yangu
mwenye nguvu,[j]
Na kutoka kwa wale
wanaonichukia; kwa
sababu walikuwa na
nguvu kuliko mimi.[k]
18 Waliendelea kunikabili
katika siku ya msiba
wangu,[l]
Lakini Yehova akawa
kama tegemeo kwa ajili
yangu.[m]
19 Naye akanitoa nje mpaka
mahali penye nafasi
tele;[n]
Alikuwa akiniokoa,
kwa sababu alikuwa
amependezwa nami.[o]
20 Yehova hunipa thawabu
kulingana na uadilifu
wangu;[p]
Hunilipa kulingana na
usafi wa mikono yangu.[q]
21 Kwa maana nimezishika
njia za Yehova,[r]

Wala kwa uovu sikuondoka
kwa Mungu wangu.[a]
22 Kwa maana maamuzi yake
yote ya hukumu yako
mbele yangu,[b]
Nazo sheria zake
sitaziondoa kutoka
kwangu.[c]
23 Nami nitajiendesha bila
kosa mbele zake,[d]
Nami nitajiepusha na
kosa.[e]
24 Yehova na anilipe
kulingana na uadilifu
wangu,[f]
Kulingana na usafi wa
mikono yangu mbele za
macho yake.[g]
25 Kwa mtu mshikamanifu
utatenda kwa
ushikamanifu;[h]
Kwa mwanamume asiye
na kosa, wewe utatenda
kwa njia isiyo na kosa;[i]
26 Kwa mtu anayebaki safi
utakuwa safi;[j]
Na kwa mpotovu utakuwa
mwenye hila;[k]
27 Kwa sababu watu
wenye kuteseka wewe
mwenyewe utawaokoa;[l]
Bali macho yenye
majivuno utayashusha.[m]
28 Kwa maana wewe
mwenyewe utaiwasha
taa yangu, Ee Yehova;[n]
Mungu wangu atafanya
giza langu liangaze.[o]
29 Kwa maana kwa
msaada wako ninaweza
kukimbiza kikundi cha
waporaji;[p]
Na kwa msaada wa
Mungu wangu ninaweza
kuupanda ukuta.[q]
30 Mungu wa kweli, njia yake
ni kamilifu;[r]
Neno la Yehova
limetakaswa.[s]

SURA 18

a Zb 119:102
b 2Sa 22:23
c Kum 8:11
d Mwa 6:9
2Sa 22:24
Zb 84:11
e Met 14:16
f Isa 3:10
Ebr 11:6
g 2Sa 22:25
Met 5:21
h Zb 97:10
Yer 3:12
i Ayu 34:11
Yer 32:19
j Da 12:10
Mt 5:8
k 2Sa 22:27
Zb 125:5
l Ayu 34:28
m Ayu 10:16
Ayu 40:11
Met 6:17
Isa 2:11
Lu 18:14
n 2Sa 22:29
Zb 132:17
o Zb 97:11
Isa 42:16
p 2Sa 5:19
Flp 4:13
Ebr 11:34
q 2Sa 22:30
r Kum 32:4
2Sa 22:31
Da 4:37
Ufu 15:3
s Zb 12:6
Zb 19:8
Zb 119:140

Safu ya 2

a Zb 18:2
Zb 84:11
Met 30:5
b 1Sa 2:2
2Sa 22:32
Zb 86:8
Isa 45:5
c Kum 32:31
d Zb 28:7
Zb 84:7
e 2Sa 22:33
Isa 26:7
f Hab 3:19
g Kum 32:13
2Sa 22:34
h Zb 144:1
i 2Sa 22:35
j Mwa 15:1
Kum 33:29
Zb 28:7
k Zb 17:7
l 2Sa 22:36
Zb 113:6
m Zb 4:1
n 2Sa 22:37
Zb 17:5
o 2Sa 22:38
p Zb 2:9
Zb 110:5
q 2Sa 22:39
Zb 110:6

Yeye ni ngao kwa wale
wote wanaomkimbilia.[a]
31 Kwa maana ni nani aliye
Mungu ila Yehova?[b]
Na ni nani aliye mwamba
ila Mungu wetu?[c]
32 Mungu wa kweli
Ndiye anayenifunga sana
mshipi wa nguvu,[d]
Naye ataifanya njia yangu
kuwa kamilifu,[e]
33 Kuifanya miguu yangu iwe
kama ya paa,[f]
Na kwenye mahali palipo
juu kwangu yeye
huendelea
kunisimamisha.[g]
34 Anaifundisha mikono
yangu kupigana vita,[h]
Na mikono yangu imepinda
upinde wa shaba.[i]
35 Nawe utanipa ngao yako
ya wokovu,[j]
Na mkono wako
mwenyewe wa kuume
utanitegemeza,[k]
Na unyenyekevu wako
mwenyewe utanifanya
kuwa mkuu.[l]
36 Utafanyiza nafasi kubwa
ya kutosha kwa ajili ya
hatua zangu zilizo chini
yangu,[m]
Navyo vifundo vya
miguu yangu hakika
havitatetemeka.[n]
37 Nitawafuatilia adui zangu
na kuwafikia;
Nami sitarudi mpaka
waangamizwe.[o]
38 Nitawavunja
vipande-vipande hivi
kwamba wasiweze
kusimama;[p]
Wataanguka chini ya
miguu yangu.[q]
39 Nawe utanifunga mshipi
wa nguvu kwa ajili ya
vita;

Utawaangusha chini yangu
wale wanaoniinukia.[a]
40 Nao adui zangu, utanipa
upande wa nyuma wa
shingo zao;[b]
Nao wale wanaonichukia
vikali,
nitawanyamazisha.[c]
41 Wanalia wapate msaada,
lakini hakuna mwokozi,[d]
Kwa Yehova, lakini yeye
hawajibu.[e]
42 Nami nitawatwanga wawe
laini kama mavumbi
mbele ya upepo;[f]
Nitawamwaga kama
matope ya barabarani.[g]
43 Utaniokoa kutokana
na watu wenye
kutafuta-tafuta makosa.[h]
Utanichagua kuwa
kiongozi wa mataifa.[i]
Watu ambao sijawajua
—watanitumikia.[j]
44 Kwa kusikia fununu tu
watanitii;[k]
Wageni watanijia
wakitetemeka.[l]
45 Wageni watakuwa dhaifu,
Nao watakuja
wakitetemeka kutoka
katika maboma yao.[m]
46 Yehova anaishi,[n] na
abarikiwe Mwamba
wangu,[o]
Na Mungu wa wokovu
wangu atukuzwe.[p]
47 Mungu wa kweli ndiye
Mpaji wa matendo ya
kisasi kwangu;[q]
Naye hutiisha vikundi vya
watu chini yangu.[r]
48 Ananiokoa kutoka kwa
adui zangu wenye
hasira;[s]
Utaniinua juu ya wale
wanaosimama dhidi
yangu,[t]
Utanikomboa kutoka kwa
mtu mwenye jeuri.[a]
49 Ndiyo sababu nitakusifu
wewe kati ya mataifa,
Ee Yehova,[b]
Nami nitalipigia jina lako
muziki.[c]
50 Yeye anafanya matendo
makuu ya wokovu kwa
ajili ya mfalme wake[d]
Na kuonyesha fadhili
zenye upendo kwa
mtiwa-mafuta wake,[e]
Kwa Daudi na kwa uzao
wake mpaka wakati
usio na kipimo.[f]

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

19 Mbingu zinatangaza
utukufu wa Mungu;[g]
Nalo anga linatangaza kazi
ya mikono yake.[h]
2 Siku moja baada ya
siku nyingine hufanya
maneno yabubujike,[i]
Na usiku mmoja baada
ya usiku mwingine
huonyesha ujuzi.[j]
3 Hakuna usemi, wala
hakuna maneno;
Sauti yao haisikiki.[k]
4 Kamba yake ya kupimia
imefika duniani pote,[l]
Na maneno yake yamefika
kwenye miisho ya nchi
yenye kuzaa.[m]
Katika hizo amewekea jua
hema,[n]
5 Nalo ni kama bwana-arusi
anapotoka katika
chumba chake cha ndoa;[o]
Linashangilia kama
mwanamume mwenye
nguvu anapokimbia
njiani.[p]

SURA 18

a 2Sa 22:40 Zb 44:5 Zb 144:2
b Mwa 49:8 Kut 23:27 Yos 10:24
c 2Sa 22:41 Zb 21:8 Zb 34:21
d 2Sa 22:42
e Ayu 35:12 Met 1:28 Isa 1:15 Yer 11:11 Yer 14:12 Mik 3:4 Zek 7:13
f 2Sa 22:43
g Isa 10:6 Zek 10:5 Mal 4:3
h 1Sa 30:6 2Sa 22:44
i 2Sa 8:3 Zb 2:8 1Ti 6:15 Ufu 19:16
j Isa 55:5 Isa 65:1 Mdo 15:14
k 2Sa 22:45
l Kum 33:29
m 2Sa 22:46 Mik 7:17
n 2Sa 22:47 Yer 10:10 1Ti 4:10
o Kum 32:4
p Kut 15:2
q Kum 32:35 2Sa 22:48 Zb 94:1 Nah 1:2 Ro 12:19
r Zb 47:3 1Ko 15:25
s Zb 59:1
t 2Sa 7:9

Safu ya 2

a 2Sa 22:49 Zb 140:1
b Kum 32:43 Zb 117:1 Isa 11:10 Ro 15:9
c 1Nya 16:9 Zb 108:3
d 1Sa 2:10 Zb 2:6 Zb 144:10
e 2Sa 7:15 1Fa 3:6 Zb 89:20
f Zb 89:36 Isa 9:7 Lu 1:33 Ufu 5:5

SURA 19

g Zb 8:3 Zb 69:34 Zb 115:15 Zb 148:3 Isa 40:22 Ro 1:20 1Ko 15:40
h Mwa 1:6 Zb 150:1 Ufu 4:11
i Zb 65:8 Zb 74:16

j Mwa 1:5; Mwa 1:14; Mwa 8:22; Zb 136:9; **k** Ayu 31:26; **l** Ayu 38:5; **m** Isa 49:6; Ro 10:18; **n** Ayu 22:14; Mhu 1:5; **o** Isa 61:10; **p** Yer 33:20.

6 Linaenda kutoka mwisho
mmoja wa mbingu,
Nao mzunguko wake
humalizikia katika ile
miisho yake mingine;[a]
Wala hakuna chochote
kilichofichwa kisiweze
kupatwa na joto lake.[b]
7 Sheria[c] ya Yehova
ni kamilifu,[d] huirudisha
nafsi.[e]
Kikumbusho[f] cha Yehova
ni chenye kutegemeka,[g]
humfanya asiye na
uzoefu awe na hekima.[h]
8 Maagizo[i] kutoka kwa
Yehova ni manyoofu,[j]
huufanya moyo
ushangilie;[k]
Amri[l] ya Yehova ni
safi,[m] huyafanya macho
yang'ae.[n]
9 Kumwogopa[o] Yehova ni
jambo safi, husimama
milele.
Maamuzi ya hukumu[p]
ya Yehova ni ya kweli;[q]
yote yameonekana kuwa
yenye uadilifu.[r]
10 Ni ya kutamaniwa kuliko
dhahabu, naam, kuliko
dhahabu safi sana;[s]
Na tamu kuliko asali[t] na
asali yenye kutiririka ya
sega.[u]
11 Pia, mtumishi wako
mwenyewe ameonywa
kupitia hayo;[v]
Katika kuyashika kuna
thawabu kubwa.[w]
12 Makosa—ni nani
anayeweza
kuyatambua?[x]
Unitangaze kuwa sina
hatia ya dhambi
zilizofichwa.[y]
13 Pia umzuie mtumishi wako
kutokana na matendo ya
kimbelembele;[z]
Usiyaache yanitawale.[a]
Hapo ndipo nitakapokuwa
kamili,[b]
Nami nitakuwa sina hatia
ya makosa mengi.
14 Maneno ya kinywa changu
na kutafakari kwa moyo
wangu[c]
Na yawe yenye kupendeza
mbele zako, Ee Yehova
Mwamba[d] wangu na
Mkombozi wangu.[e]

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

20 Yehova na akujibu siku
ya taabu.[f]
Jina la Mungu wa Yakobo
na likulinde.[g]
2 Na atume msaada wako
kutoka katika mahali
patakatifu,[h]
Na kukutegemeza kutoka
Sayuni.[i]
3 Na akumbuke matoleo
yako yote ya zawadi,[j]
Naye na ayakubali matoleo
yako ya kuteketezwa
kuwa ni mafuta.[k] *Sela*.
4 Na akupe kulingana na
moyo wako,[l]
Naye na alitimize kusudi
lako lote.[m]
5 Tutapiga vigelegele kwa
shangwe kwa sababu ya
wokovu wako,[n]
Nasi tutainua bendera zetu
katika jina la Mungu
wetu.[o]
Yehova na atimize maombi
yako yote.[p]
6 Sasa najua kwamba hakika
Yehova humwokoa
mtiwa-mafuta wake.[q]
Humjibu kutoka katika
mbingu zake takatifu[r]

SURA 19

a Zb 104:19
b Mwa 31:40
Isa 49:10
Mt 20:12
c Kum 33:4
Zb 1:2
Zb 78:1
d Zb 119:72
Mt 5:17
Lu 2:22
Ro 2:13
Ro 7:14
Ro 7:22
Ro 9:31
e 2Sa 16:12
1Fa 8:47
Zb 23:3
Eze 18:27
Eze 33:15
Ro 10:5
f Zb 119:111
Zb 119:129
Zb 132:12
2Pe 3:1
g 2Fa 17:15
Zb 93:5
h Met 1:5
2Ti 3:15
i Kum 1:26
1Sa 12:14
Zb 111:7
j Zb 33:4
k 2Nya 24:10
Zb 40:8
Zb 119:7
l Kum 6:1
Met 4:4
Mt 15:3
m Ne 9:13
n Zb 13:3
Met 6:23
Mt 6:22
o Kum 10:12
Met 1:7
Mal 3:16
p Kut 21:1
Hes 15:35
Ne 9:13
Zb 119:137
q Zb 119:160
Ufu 16:7
r Kum 4:8
s Zb 119:127
Met 8:10
t Zb 119:103
Met 16:24
u 1Sa 14:27
v 2Nya 19:10
Zb 119:11
w Zb 119:165
Met 11:18
x Zb 40:12
1Ko 4:4
y Law 4:2
Zb 90:8
z Mwa 20:6
Kum 17:12
1Sa 15:23
2Sa 6:7
2Nya 26:16

Safu ya 2

a Zb 119:133
b Isa 38:3
c Zb 49:3
Zb 51:15
Zb 77:12
Zb 143:5
Flp 4:8
d Zb 18:2
e Ayu 19:25
Met 23:11
Isa 43:14
Isa 44:6

SURA 20 f Mwa 35:3; 2Sa 4:9; g Zb 9:10; Met 18:10; h 2Nya 20:8; i 2Sa 5:7; Zb 50:2; Zb 134:3; Isa 12:6; j Mdo 10:4; k Law 9:24; l Nya 21:26; 2Nya 7:1; l Zb 21:2; m Met 20:5; n Zb 35:9; Zb 51:14; Zb 59:16; Lu 1:47; o 1Sa 17:45; p Mt 7:7; q Zb 2:2; Zb 105:15; Lu 18:7; r 1Fa 8:30; Zb 18:9.

Kwa matendo ya kuokoa
yenye nguvu ya mkono
wake wa kuume.[a]
7 Wengine hutaja kuhusu
magari na wengine
kuhusu farasi,[b]
Lakini sisi, tutataja
kuhusu jina la Yehova
Mungu wetu.[c]
8 Hao wamevunjika na
kuanguka;[d]
Lakini sisi, tumesimama,
ili tupate kurudishwa.[e]
9 Ee Yehova, umwokoe
mfalme![f]
Yeye atatujibu siku
ambayo tutaita.[g]

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

21 Ee Yehova, mfalme
hushangilia katika
nguvu zako;[h]
Na katika wokovu wako
jinsi anavyotaka kuwa
na shangwe sana![i]
2 Tamaa ya moyo wake
umempa,[j]
Na matakwa ya midomo
yake hukuyazuilia.[k]
Sela.
3 Kwa maana ulikutana
naye ukiwa na baraka
za mema,[l]
Na kumvika taji la
dhahabu safi kichwani.[m]
4 Alikuomba uhai. Ukampa
huo,[n]
Urefu wa siku mpaka
wakati usio na kipimo,
naam, milele.[o]
5 Utukufu wake ni mkuu
katika wokovu wako.[p]
Heshima na fahari
unaweka juu yake.[q]
6 Kwa maana umemfanya
abarikiwe sana milele;[r]
Unamfanya afurahie kwa
shangwe mbele za uso
wako.[s]

SURA 20

a Zb 17:7
b Zb 33:17
Met 21:31
Isa 31:1
Ho 1:7
c 2Nya 14:11
2Nya 20:12
2Nya 32:8
d Amu 5:31
e Zb 125:1
f Zb 18:50
g Zb 44:4

SURA 21

h Zb 63:11
i Zb 28:7
j Zb 2:8
k Zb 20:4
l 2Nya 6:41
Zb 31:19
m 2Sa 12:30
n Zb 13:3
Zb 61:6
o Zb 89:29
Zb 91:16
p 2Sa 7:9
Ebr 8:1
q Da 7:14
r Zb 72:17
s Zb 16:11
Zb 45:7
Mdo 2:28

Safu ya 2

a 1Sa 30:6
Mt 27:43
Ebr 2:13
b Zb 16:8
c Zb 2:9
d Mhu 3:8
Mal 4:1
2Th 1:8
e Kum 32:22
Zb 110:5
f 1Fa 13:34
Zb 9:5
Zb 37:28
Mt 25:46
g Zb 109:13
Isa 14:20
h Zb 5:10
Zb 34:16
i Zb 2:1
Zb 83:4
j Zb 9:3
Zb 56:9
k Zb 7:13
Zb 64:7
l Zb 46:10
m Ufu 11:17
Ufu 15:3
Ufu 18:20

SURA 22

n Zb 22:16
Zb 31:14
Mt 27:46
Mk 15:34
o Zb 26:9
Ebr 5:7
p Ayu 3:24
Zb 38:8

7 Kwa maana mfalme
anategemea Yehova,[a]
Naam, fadhili zenye
upendo za Aliye Juu
Zaidi. Hatatikiswa.[b]
8 Mkono wako utawapata
adui zako wote;[c]
Mkono wako wa
kuume utawapata wale
wanaokuchukia.
9 Utawafanya wawe kama
tanuru yenye moto
wakati wako uliowekwa
wa kukaza uangalifu
wako;[d]
Yehova atawameza katika
hasira yake, na moto
utawateketeza.[e]
10 Utaangamiza wazaliwa wao
kutoka duniani,[f]
Na uzao wao kutoka kati
ya wana wa binadamu.[g]
11 Kwa maana
wamekuelekezea
mabaya;[h]
Wametunga mawazo
wasiyoweza kutimiza.[i]
12 Kwa maana utawafanya
wageuze migongo yao
kwa kukimbia[j]
Kwa nyuzi za upinde wako
ambazo unatayarisha
dhidi ya nyuso zao.[k]
13 Na utukuzwe katika nguvu
zako, Ee Yehova.[l]
Tutaimba na kuzipigia
muziki nguvu zako.[m]

Kwa kiongozi juu ya Paa wa
Mapambazuko. Muziki wa Daudi.

22 Mungu wangu, Mungu
wangu, kwa nini
umeniacha?[n]
Kwa nini uko mbali
usiniokoe,[o]
Mbali na maneno ya
mngurumo wangu?[p]
2 Ee Mungu wangu, mimi
huendelea kuita wakati

wa mchana, nawe
huitiki;[a]
Na wakati wa usiku, wala
sinyamazi.[b]
3 Lakini wewe ni mtakatifu,[c]
Unayekaa juu ya sifa za
Israeli.[d]
4 Baba zetu walikutegemea
wewe;[e]
Walikutegemea, nawe
ukaendelea kuwaokoa.[f]
5 Walikulilia,[g] nao wakawa
salama;[h]
Walikutegemea, nao
hawakuona aibu.[i]
6 Lakini mimi ni mdudu,[j]
wala si mtu,
Shutuma kwa
wanadamu na mwenye
kudharaulika kwa watu.[k]
7 Wale wote wanaoniona
mimi, hunidharau;[l]
Wanaendelea kufungua
vinywa vyao wazi,
wanaendelea kutikisa
vichwa vyao:[m]
8 "Yeye alijitia mikononi
mwa Yehova.[n] Acha
Yeye amwokoe![o]
Na amkomboe, kwa
kuwa yeye amependezwa
naye!"[p]
9 Kwa maana Wewe ndiye
uliyenitoa tumboni,[q]
Wewe ndiye unayenifanya
niwe na tegemeo
nilipokuwa kwenye
maziwa ya mama yangu.[r]
10 Nimetupwa kwako kutoka
tumbo la uzazi;[s]
Kutoka katika tumbo
la mama yangu wewe
umekuwa Mungu
wangu.[t]
11 Usikae mbali nami, kwa
sababu taabu iko karibu,[u]
Kwa sababu hakuna
msaidizi mwingine.[v]

SURA 22

a Zb 42:3
Zb 88:1
b Lu 18:7
c Isa 6:3
Yoh 17:11
1Pe 1:15
d Kum 10:21
Zb 65:1
e Mwa 15:6
Ebr 11:33
f Kut 14:13
g Zb 99:6
Zb 106:44
h 1Ko 10:13
i Zb 25:2
Isa 49:23
Ro 10:11
j Ayu 25:6
Isa 41:14
k Zb 31:11
Isa 53:3
Yoh 7:15
l Zb 35:16
Mt 5:11
Mt 9:24
Lu 16:14
m Ayu 16:4
Zb 44:14
Zb 109:25
Mt 27:39
n Zb 37:5
o Mt 27:43
Lu 23:35
p Zb 18:19
Zb 91:14
q Zb 71:6
Zb 139:16
r Lu 11:27
s Isa 46:3
t Isa 49:1
Lu 1:42
Ga 1:15
u Zb 10:1
Ebr 5:7
v Zb 72:12
Lu 23:46

Safu ya 2

a Zb 68:30
b Isa 53:7
Eze 39:18
Amo 4:1
Mt 27:1
c Ayu 16:10
Zb 35:21
Omb 2:16
Mt 26:4
d Zb 57:4
1Pe 5:8
e Yos 7:5
f Da 5:6
Lu 22:44
g Ayu 23:16
Yoh 12:27
h Kum 20:8
Mt 26:38
Mk 14:33
i Met 17:22
j Omb 4:4
Yoh 19:28
k Mwa 3:19
Zb 30:9
Isa 53:12
1Ko 15:4
l Zb 59:6
Lu 22:63
Flp 3:2
Ufu 22:15
m Zb 86:14
Lu 11:53
n Isa 53:7
Mt 27:35
Yoh 20:25
o Zb 34:20
Yoh 19:36

12 Ng'ombe-dume wengi
wachanga
wamenizingira;[a]
Wale wenye nguvu wa
Bashani
wamenizunguka.[b]
13 Wamefungua vinywa vyao
dhidi yangu,[c]
Kama simba anayerarua
vipande-vipande na
kunguruma.[d]
14 Nimemwagwa kama maji,[e]
Na mifupa yangu yote
imetenganishwa.[f]
Moyo wangu umekuwa
kama nta;[g]
Umeyeyuka ndani katika
sehemu zangu za ndani.[h]
15 Nguvu zangu zimekauka
kama kigae cha udongo,[i]
Na ulimi wangu
umefanywa ushikamane
na ufizi wangu;[j]
Nawe unaniweka katika
mavumbi ya kifo.[k]
16 Kwa maana mbwa
wamenizingira;[l]
Kusanyiko la
watenda-maovu
limenizunguka.[m]
Wako kwenye mikono
yangu na miguu yangu
kama simba.[n]
17 Naweza kuhesabu mifupa
yangu yote.[o]
Wao hutazama, hunikazia
macho.[p]
18 Wanagawana mavazi
yangu,[q]
Nao wanalipigia kura vazi
langu.[r]
19 Lakini wewe, Ee Yehova,
usikae mbali.[s]
Ewe nguvu zangu,[t] ufanye
haraka kuja kunisaidia.[u]

p Mt 27:36; Lu 23:35; **q** Yoh 19:24; **r** Mk 15:24; **s** Zb 10:1; **t** Zb 18:1; **u** Zb 40:13.

20 Uikomboe nafsi yangu
kutokana na upanga,[a]
Nafsi yangu ya pekee
kutokana na wayo wa
mbwa;[b]
21 Uniokoe kutokana na
kinywa cha simba,[c]
Na unijibu na kuniokoa
kutokana na pembe za
ng'ombe-mwitu.[d]
22 Nitalitangaza jina lako[e]
kwa ndugu zangu;[f]
Katikati ya kutaniko
nitakusifu wewe.[g]
23 Ninyi mnaomwogopa
Yehova, msifuni![h]
Enyi nyote mlio uzao wa
Yakobo, mtukuzeni![i]
Na mwogopeni yeye, enyi
nyote mlio uzao wa
Israeli.[j]
24 Kwa maana hakudharau[k]
Wala kuchoshwa na
mateso ya mwenye
kuteseka;[l]
Naye hakumficha uso
wake,[m]
Naye alipomlilia amsaidie
alisikia.[n]
25 Kutoka kwako sifa yangu
itakuwa katika kutaniko
kubwa;[o]
Nadhiri zangu nitazitimiza
mbele ya wale
wanaomwogopa.[p]
26 Wapole watakula na
kushiba;[q]
Wale wanaomtafuta
watamsifu Yehova.[r]
Mioyo yenu na iishi milele.[s]
27 Miisho yote ya dunia
itakumbuka na kurudi
kwa Yehova.[t]
Na familia zote za mataifa
zitainama mbele zako.[u]
28 Kwa maana ufalme ni wa
Yehova,[v]
Naye anayatawala
mataifa.[a]
29 Wote walio wanono wa
dunia watakula na
kuinama;[b]
Wote wanaoenda chini
mavumbini watainama
mbele zake,[c]
Wala hakuna
atakayeihifadhi hai
nafsi yake.[d]
30 Uzao utamtumikia;[e]
Kizazi hicho kitatangaziwa
juu ya Yehova.[f]
31 Watakuja na kusema juu
ya uadilifu wake[g]
Kwa kikundi cha watu
kitakachozaliwa,
kwamba ni yeye
amefanya hilo.[h]

Muziki wa Daudi.

23 Yehova ni Mchungaji
wangu.[i]
Sitakosa chochote.[j]
2 Ananilaza katika malisho
yenye majani mengi;[k]
Ananiongoza kando ya
mahali pa kupumzika
palipo na maji ya
kutosha.[l]
3 Anaiburudisha nafsi
yangu.[m]
Ananiongoza katika
mapito ya uadilifu kwa
ajili ya jina lake.[n]
4 Hata ingawa ninatembea
katika bonde lenye
kivuli kizito,[o]
Siogopi chochote kibaya,[p]
Kwa maana wewe uko
pamoja nami;[q]
Fimbo yako na gongo
lako ndivyo vitu
vinavyonifariji.[r]

SURA 22

a Zb 17:13; Zb 37:17
b Zb 22:16
c Zb 35:17; 2Ti 4:17
d Kum 33:17; Yoh 8:59; Mdo 4:27
e Yoh 17:6; Ebr 2:12
f Mt 12:49; Yoh 20:17; Ro 8:29; Ebr 2:11; Ebr 2:17
g Zb 40:9; Ebr 2:12
h Zb 135:20; Lu 1:50; Mdo 4:24
i Zb 50:15; Zb 50:23; Lu 2:20; 1Ko 6:20; Ufu 15:4
j Kum 6:13
k Zb 69:33
l Zb 34:6
m Hes 6:25
n Ebr 5:7
o Zb 35:18; Zb 40:10; Zb 107:32; Zb 111:1
p Mhu 5:4
q Zb 37:11; Isa 65:13
r Sef 2:3
s Yoh 4:14
t Isa 66:20
u Mwa 22:18; Ufu 7:9; Ufu 15:4
v 1Nya 29:11; Oba 21; Ufu 11:17

Safu ya 2

a Zb 47:7; Zek 14:9
b Zb 45:12
c Isa 26:19; Flp 2:10
d Zb 49:7
e Isa 53:10
f 1Pe 2:9
g Ro 1:17; Ro 3:22
h Zb 78:6; Zb 102:18

SURA 23

i Zb 80:1; Yer 23:3; Eze 34:12; 1Pe 2:25
j Zb 34:9; Zb 84:11; Mt 6:33; Flp 4:19; Ebr 13:5
k Eze 34:14; Mt 4:4
l Ayu 34:29; Eze 34:13
m Zb 19:7; Zb 51:12
n Zb 5:8; Zb 31:3; Met 8:20
o Ayu 10:21; Ayu 38:17; Zb 44:19; Mt 4:16; Lu 1:79;
p Zb 3:6; Zb 27:1; Isa 41:10;
q Isa 43:2; Ro 8:31;
r Mik 7:14.

5 Mbele yangu wewe
unatayarisha meza
mbele ya wale
wanaonionyesha uadui.[a]
Umepaka kichwa changu
mafuta;[b]
Kikombe changu
kimejazwa vizuri.[c]
6 Kwa hakika wema na
fadhili zenye upendo
zitanifuata siku zote
za maisha yangu;[d]
Nami nitakaa katika
nyumba ya Yehova
siku nyingi.[e]

Ya Daudi. Muziki.

24 Dunia na vyote
vinavyoijaza ni vya
Yehova,[f]
Nchi yenye kuzaa na
wale wanaokaa ndani
yake.[g]
2 Kwa maana yeye ameiweka
imara juu ya bahari,[h]
Naye huiweka imara juu
ya mito.[i]
3 Ni nani anayeweza
kuupanda mlima wa
Yehova,[j]
Na ni nani anayeweza
kusimama katika mahali
pake patakatifu?[k]
4 Yeyote asiye na hatia
katika mikono yake na
aliye safi moyoni,[l]
Ambaye hajaitendea nafsi
Yangu kwa ubatili
mtupu,[m]
Wala kuapa kwa
udanganyifu.[n]
5 Atachukua baraka kutoka
kwa Yehova[o]
Na uadilifu kutoka kwa
Mungu wake wa
wokovu.[p]
6 Hiki ndicho kizazi cha
wale wanaomtafuta,
Cha wale wanaoutafuta
uso wako, Ee Mungu wa
Yakobo.[a] *Sela*.
7 "Inueni vichwa vyenu,
enyi malango,[b]
Na mjiinue, enyi miingilio
ya kudumu,[c]
Ili Mfalme mtukufu apate
kuingia!"[d]
8 "Basi, Mfalme huyo
mtukufu ni nani?"[e]
"Yehova mwenye nguvu
na mwenye uwezo,[f]
Yehova mwenye uwezo
katika vita."[g]
9 "Inueni vichwa vyenu,
enyi malango;[h]
Naam, viinueni juu,
enyi miingilio ya
kudumu,
Ili Mfalme mtukufu apate
kuingia!"[i]
10 "Basi, yeye ni nani, huyo
Mfalme mtukufu?"
"Yehova wa majeshi
—yeye ndiye Mfalme
mtukufu."[j] *Sela*.

Ya Daudi.

א [*'A'leph*]

25 Kwako wewe, Ee
Yehova, naiinua nafsi
yangu.[k]

ב [*Behth*]

2 Ee Mungu wangu,
nimekutegemea wewe;[l]
Ee nisione aibu.
Adui zangu na wasishangilie
juu yangu.[m]

ג [*Gi'mel*]

3 Pia, hakuna yeyote kati ya
wale wanaokutumainia
atakayeona aibu.[n]
Wale wanaotenda kwa hila
bila kupata mafanikio
wataona aibu.[o]

SURA 23

a Zb 22:26
Zb 31:19
b Zb 92:10
Lu 7:46
Yak 5:14
c Zb 16:5
d Zb 103:17
Efe 5:9
e Zb 15:1
Zb 27:4
Zb 65:4
Zb 84:4
Zb 122:1
Lu 2:37
Ufu 21:3

SURA 24

f Kut 9:29
Kut 19:5
Kum 10:14
1Nya 29:11
Ayu 41:11
1Ko 10:26
g Zb 89:11
Zb 98:7
h Mwa 1:9
Zb 136:6
i Ayu 38:11
Zb 96:10
Zb 104:5
Yer 5:22
j Zb 15:1
Isa 2:2
k Ro 11:35
l 2Sa 22:21
Zb 37:3
Isa 33:15
Mt 5:8
m Mwa 50:20
Ro 8:29
n Zb 34:13
Mal 3:5
o Zb 128:5
Mal 3:10
p Zb 68:19
Isa 12:2
Tit 2:10

Safu ya 2

a Zb 27:8
Zb 105:4
b Zb 118:19
c Isa 26:2
d 2Sa 6:15
Zb 48:2
Zb 97:6
e Zb 99:1
f Zb 93:1
Isa 42:13
1Ti 1:17
g Kut 15:3
1Sa 17:47
2Nya 20:15
Isa 59:17
h Zb 118:19
Zb 122:2
i Zb 68:16
j 1Nya 29:11
Zb 145:1
Isa 6:5
Ufu 1:8

SURA 25

k Zb 86:4
Zb 143:8
l Isa 26:3
Ro 10:11
m Zb 13:4
Zb 35:19
Zb 41:11
n Zb 69:6
o Zb 31:17
Zb 71:13

ד [*Da´leth*]

4 Nijulishe njia zako, Ee Yehova;[a]
Nifundishe mapito yako mwenyewe.[b]

ה [*He'*]

5 Nitembeze katika kweli yako na kunifundisha,[c]
Kwa maana wewe ni Mungu wangu wa wokovu.[d]

ו [*Waw*]

Nimekutumainia mchana kutwa.[e]

ז [*Za´yin*]

6 Ukumbuke rehema zako,[f] Ee Yehova, na fadhili zako zenye upendo,[g]
Kwa maana ni za tangu wakati usio na kipimo.[h]

ח [*Chehth*]

7 Usizikumbuke dhambi za ujana wangu na maasi yangu.[i]
Unikumbuke kulingana na fadhili zako zenye upendo,[j]
Kwa ajili ya wema wako, Ee Yehova.[k]

ט [*Tehth*]

8 Yehova ni mwema na mnyoofu.[l]
Ndiyo sababu yeye huwafundisha watenda-dhambi katika ile njia.[m]

י [*Yohdh*]

9 Atawafanya wapole watembee katika uamuzi wake wa hukumu,[n]
Naye atawafundisha wapole njia yake.[o]

כ [*Kaph*]

10 Mapito yote ya Yehova ni fadhili zenye upendo na ukweli
Kwa wale wanaoshika agano lake[a] na vikumbusho vyake.[b]

ל [*La´medh*]

11 Kwa ajili ya jina lako, Ee Yehova,[c]
Usamehe kosa langu, kwa maana ni kubwa.[d]

מ [*Mem*]

12 Sasa, ni nani anayemwogopa Yehova?[e]
Atamfundisha katika njia ambayo yeye ataichagua.[f]

נ [*Nun*]

13 Nafsi yake itakaa katika wema,[g]
Na uzao wake mwenyewe utaimiliki dunia.[h]

ס [*Sa´mekh*]

14 Urafiki wa karibu pamoja na Yehova ni wa wale wanaomwogopa,[i]
Pia agano lake, ili kuwafanya walijue.[j]

ע [*'A´yin*]

15 Macho yangu yanamwelekea Yehova daima,[k]
Kwa maana yeye ndiye huitoa miguu yangu katika wavu.[l]

פ [*Pe'*]

16 Unielekezee uso wako, na unionyeshe kibali;[m]
Kwa maana mimi niko peke yangu nami ni mwenye kuteseka.[n]

צ [*Tsa·dheh´*]

17 Taabu za moyo wangu zimeongezeka;[o]
Uniondoe katika mikazo iliyo juu yangu.[p]

SURA 25

a Kut 33:13
Zb 5:8
Zb 86:11
Zb 143:8
b Zb 27:11
c Zb 43:3
d Zb 24:5
Zb 88:1
e Zb 22:2
f 2Nya 6:42
Zb 98:3
Zb 103:17
Isa 63:15
g Kut 34:6
Zb 69:16
Isa 55:3
Yer 33:11
h Zb 136:1
Lu 1:50
i Ayu 13:26
Yer 3:25
j Zb 6:4
Zb 51:1
k Kut 33:19
Zb 27:13
l Zb 92:15
Zb 119:68
Zb 145:9
Nah 1:7
Zek 9:17
Mdo 14:17
m Zb 119:33
Isa 30:20
Mik 4:2
n Sef 2:3
o Zb 32:8

Safu ya 2

a Kum 29:1
b Zb 19:7
c Zb 31:3
Zb 79:9
Zb 109:21
Zb 143:11
Eze 36:22
Da 9:19
Mt 6:9
d Zb 103:3
e Zb 111:10
Mdo 10:2
f Zb 37:23
g Zb 31:19
Zek 9:17
h Zb 37:11
i Mwa 18:17
Met 3:32
Amo 3:7
Yoh 15:15
j Mwa 22:17
k Zb 121:1
Zb 123:1
Zb 141:8
l Zb 31:4
Zb 91:3
Zb 124:7
2Ti 2:26
m Zb 69:16
Zb 86:16
n Zb 143:4
o Zb 73:21
p Zb 107:28

ר [*Rehsh*]

18 Uone mateso yangu na
taabu yangu,[a]
Na unisamehe dhambi
zangu zote.[b]
19 Uone jinsi adui zangu
wamekuwa wengi,[c]
Nao wamenichukia kwa
chuki yenye jeuri.[d]

ש [*Shin*]

20 Uilinde nafsi yangu na
kunikomboa.[e]
Nisione aibu, kwa maana
nimekukimbilia wewe.[f]

ת [*Taw*]

21 Utimilifu na unyoofu na
zinilinde,[g]
Kwa maana
nimekutumainia wewe.[h]
22 Ee Mungu, mkomboe
Israeli kutoka katika
taabu zake zote.[i]

Ya Daudi.

26 Unihukumu,[j] Ee
Yehova, kwa maana
nimetembea katika
utimilifu wangu,[k]
Nami nimemtumaini
Yehova, nisipate
kutikisika.[l]
2 Unichunguze, Ee Yehova,
na kunijaribu;[m]
Usafishe figo zangu na
moyo wangu.[n]
3 Kwa maana fadhili zako
zenye upendo ziko mbele
ya macho yangu,
Nami nimetembea katika
kweli yako.[o]
4 Sikuketi na watu
wasiosema kweli;[p]
Wala siingii pamoja na
wale wanaoficha jinsi
walivyo.[q]
5 Nimelichukia kutaniko la
watenda-maovu,[r]
Wala siketi pamoja na
waovu.[a]
6 Nitaiosha mikono yangu
katika kutokuwa na
hatia,[b]
Nami nitatembea
nikizunguka madhabahu
yako, Ee Yehova,[c]
7 Ili kufanya utoaji shukrani
usikiwe kwa sauti
kubwa,[d]
Na kutangaza kazi zako
zote za ajabu.[e]
8 Yehova, nimependa makao
ya nyumba yako[f]
Na mahali ambapo
utukufu wako hukaa.[g]
9 Usiiondoe nafsi
yangu pamoja na
watenda-dhambi,[h]
Wala uhai wangu pamoja
na watu wenye hatia ya
damu,[i]
10 Ambao mikononi mwao
wana mwenendo
mpotovu,[j]
Na ambao mkono wao wa
kuume umejaa rushwa.[k]
11 Mimi nami nitatembea
katika utimilifu wangu.[l]
Ee unikomboe[m] na
kunionyesha kibali.[n]
12 Mguu wangu utasimama
mahali tambarare;[o]
Kati ya makundi
yaliyokutanika
nitambariki Yehova.[p]

Ya Daudi.

27 Yehova ni nuru yangu[q]
na wokovu wangu.[r]
Nitamwogopa nani?[s]
Yehova ni ngome ya uhai
wangu.[t]
Nitamhofu nani?[u]
2 Watenda-maovu
walipokuja karibu juu

SURA 25
a 2Sa 16:12; Zb 119:153
b Zb 32:5; Zb 51:9
c Zb 38:19
d Zb 37:12
e Zb 17:8; Zb 121:7
f Zb 71:1
g Zb 41:12
h Zb 37:34; Ro 15:13
i Zb 130:8

SURA 26
j Zb 7:8
k 2Fa 20:3; Met 20:7
l Zb 21:7; Zb 37:31; Met 3:6; Met 29:25
m Mwa 22:1; Zb 7:9
n Zb 17:3; Zb 66:10; Zek 13:9
o 2Fa 20:3; Zb 43:3; Zb 86:11
p Met 13:20; Yer 15:17
q Met 12:11; 1Ko 15:33
r Zb 31:6; Zb 139:21

Safu ya 2
a Zb 1:1
b Zb 51:2; Zb 73:13; Isa 1:16; Mt 27:24
c Zb 43:4
d Zb 50:23; Zb 95:2
e Zb 107:22
f 1Sa 3:3; 1Nya 16:1; Zb 27:4; Zb 84:10
g 2Nya 5:14; Zb 63:2
h 1Sa 25:29
i Zb 51:14
j Ga 5:19; 2Pe 2:7
k Kum 16:19; 1Sa 8:3; Isa 1:23; Eze 22:12; Amo 5:12
l Lu 1:6
m Zb 69:18
n Ne 13:14; Zb 40:2
o 1Sa 2:9; Met 10:9
p Zb 68:26; Zb 107:32; Zb 111:1

SURA 27
q Ayu 29:3; Zb 36:9; Zb 43:3; Zb 119:105
r Kut 15:2; Zb 68:19
s Zb 23:4
t Zb 62:6; Isa 12:2; Flp 4:13;
u Zb 36:1; Ro 8:31; Ebr 13:6.

yangu ili wapate kuila
nyama yangu,[a]
Wao wakiwa ni wapinzani
wangu na adui zangu,[b]
Wao walijikwaa na
kuanguka.[c]
3 Hata kambi ijapopiga hema
dhidi yangu,[d]
Moyo wangu hautaogopa.[e]
Vita vijapozuka dhidi
yangu,[f]
Bado nitakuwa na tegemeo
wakati huo.[g]
4 Nimemwomba Yehova
jambo moja[h]—
Ndilo nitakalolitafuta,[i]
Kwamba nipate kukaa
katika nyumba ya
Yehova siku zote za
maisha yangu,[j]
Ili kuuona uzuri wa
Yehova[k]
Na kulitazama kwa
uthamini hekalu lake.[l]
5 Kwa maana atanificha
mafichoni mwake katika
siku ya msiba;[m]
Atanificha katika mahali
pa siri pa hema lake;[n]
Ataniweka juu kwenye
mwamba.[o]
6 Na sasa kichwa
changu kitakuwa juu,
juu ya adui zangu
wanaonizunguka
pande zote;[p]
Nami nitatoa kwenye
hema lake dhabihu za
vigelegele vya shangwe;[q]
Nitamwimbia Yehova na
kumpigia muziki.[r]
7 Usikie, Ee Yehova,
ninapoita kwa sauti
yangu,[s]
Na unionyeshe kibali na
kunijibu.[t]
8 Moyo wangu umesema hivi
juu yako: "Utafuteni uso
wangu."[u]
Nitautafuta uso wako,
Ee Yehova.[a]
9 Usinifiche uso wako.[b]
Usimgeuzie mbali
mtumishi wako kwa
hasira.[c]
Uwe msaada wangu.[d]
Usinitupe wala usiniache,
Ee Mungu wa wokovu
wangu.[e]
10 Hata ikiwa baba yangu
na mama yangu
wangeniacha,[f]
Yehova mwenyewe
angenichukua.[g]
11 Unifundishe njia yako,
Ee Yehova,[h]
Na uniongoze katika njia
ya unyoofu kwa sababu
ya adui zangu.
12 Usinitie mikononi mwa
nafsi ya wapinzani
wangu;[i]
Kwa maana dhidi yangu
wamesimama mashahidi
wa uwongo,[j]
Na yeye anayetokeza
jeuri.[k]
13 Kama nisingalikuwa na
imani katika kuuona
wema wa Yehova katika
nchi ya walio hai[l]—!
14 Mtumaini Yehova;[m] uwe
hodari na moyo wako
uwe na nguvu.[n]
Naam, mtumaini Yehova.[o]

Ya Daudi.

28 Mimi huendelea kukuita
wewe, Ee Yehova.[p]
Ee Mwamba wangu, usiwe
kwangu kama kiziwi,[q]
Ili usininyamazie[r]
Nami nisilazimike kuwa
kama wale wanaoshuka
chini shimoni.[s]

SURA 27

a Zb 14:4; Zb 22:16
b Zb 18:40
c Zb 18:38
d Zb 3:6
e 2Nya 20:15
f 2Nya 32:7
g Zb 84:12
h Lu 10:42
i Yer 29:13; Da 9:3; Mt 7:7
j Zb 15:1; Zb 23:6; Zb 65:4; Lu 2:37
k Zb 16:11; Zb 50:2; Zb 63:2; Zb 90:17
l 1Sa 3:3; 1Nya 16:1; Zb 26:8; Ebr 12:16
m Zb 31:20; Zb 32:7; Zb 57:1; Sef 2:3
n Zb 61:4; Zb 119:114
o Zb 40:2
p 2Sa 7:9; Zb 3:3
q Zb 107:22; Ebr 13:15
r Efe 5:19
s Zb 4:1; Zb 130:2
t Zb 5:2; Zb 119:58
u Zb 24:6; Zb 105:4; Sef 2:3

Safu ya 2

a Zb 63:1
b Zb 69:17; Zb 143:7; Isa 59:2
c Isa 50:1
d 1Sa 7:12; Zb 46:1
e Zb 38:21; Zb 88:1
f Zb 69:8; Mt 10:21
g Isa 40:11; Isa 49:15
h 1Fa 8:36; Zb 25:4; Zb 86:11; Isa 30:20; Isa 54:13
i Zb 31:8; Zb 35:25; Zb 41:2; Zb 41:11
j Zb 35:11; Mt 26:59; Mdo 6:11
k Mdo 9:1
l Ayu 33:30; Yer 11:19; Eze 26:20
m Zb 25:3
n Zb 31:24; Isa 40:31
o Zb 62:5; Zb 130:5; Ro 15:13

SURA 28

p Zb 18:3
q Kum 32:4; Zb 42:9; Isa 26:4;
r Zb 35:22; Zb 83:1;
s Ayu 33:28; Zb 30:9; Zb 69:15; Isa 38:18.

2 Uisikie sauti ya kusihi
kwangu ninapokulilia
unisaidie,
Wakati ninapoinua
mikono[a] yangu katika
chumba cha ndani kabisa
cha mahali pako
patakatifu.[b]
3 Usinikokote pamoja na
watu waovu na pamoja
na wanaotenda mambo
yenye kuumiza,[c]
Wale wanaosema amani
na wenzao[d] lakini ambao
katika mioyo yao mna
jambo lililo baya.[e]
4 Uwape kulingana na
matendo yao[f]
Na kulingana na ubaya
wa mazoea yao.[g]
Uwape kulingana na kazi
ya mikono yao.[h]
Uwalipe matendo yao
wenyewe.[i]
5 Kwa maana hawajali
utendaji wa Yehova,[j]
Wala kazi ya mikono yake.[k]
Yeye atawabomoa wala
hatawajenga.
6 Yehova na abarikiwe, kwa
maana ameisikia sauti
ya kusihi kwangu.[l]
7 Yehova ni nguvu[m] zangu
na ngao[n] yangu.
Moyo wangu
umemtegemea yeye,[o]
Nami nimesaidiwa, hivi
kwamba moyo wangu
unashangilia,[p]
Nami nitamsifu kwa
wimbo wangu.[q]
8 Yehova ni nguvu kwa watu
wake,[r]
Naye ni ngome ya wokovu
mkuu wa mtiwa-mafuta
wake.[s]
9 Uwaokoe watu wako, na
kuubariki urithi wako;[t]
Na uwachunge na
kuwabeba mpaka wakati
usio na kipimo.[a]

Muziki wa Daudi.

29 Mhesabieni Yehova,
enyi wana wa wenye
nguvu,
Mhesabieni Yehova
utukufu na nguvu.[b]
2 Mhesabieni Yehova
utukufu wa jina lake.[c]
Mwinamieni Yehova katika
pambo takatifu.[d]
3 Sauti ya Yehova iko juu ya
maji;[e]
Mungu mtukufu[f]
mwenyewe
amenguruma.[g]
Yehova yuko juu ya maji
mengi.[h]
4 Sauti ya Yehova ina nguvu;[i]
Sauti ya Yehova ni yenye
fahari.[j]
5 Sauti ya Yehova inaivunja
mierezi;
Naam, Yehova anaivunja
vipande-vipande mierezi
ya Lebanoni,[k]
6 Naye huifanya irukeruke
kama ndama,[l]
Lebanoni na Sirioni[m] kama
wana wa ng'ombe-mwitu.
7 Sauti ya Yehova inapasua
kwa miali ya moto;[n]
8 Sauti ya Yehova huifanya
nyika itetemeke,[o]
Yehova huifanya nyika ya
Kadeshi[p] itetemeke.
9 Sauti ya Yehova huwafanya
paa watetemeke kwa
maumivu ya kuzaa[q]
Na kuivua kabisa misitu.[r]
Na katika hekalu lake
kila mmoja anasema:
"Utukufu!"[s]
10 Yehova ameketi juu ya
gharika;[t]

SURA 28

a 2Nya 6:13
b Zb 5:7
c Hes 16:26
Zb 26:9
d Zb 62:4
Yer 9:8
e Zb 7:14
Zb 36:4
Met 26:25
f Zb 59:12
Yer 18:22
2Ti 4:14
g Zb 21:10
h Zb 62:12
Mt 25:45
Ufu 22:12
i 2Th 1:6
j Ayu 34:27
Isa 5:12
k Zb 8:3
Zb 19:1
Isa 40:26
l Zb 66:20
m Isa 12:2
Efe 6:10
n Mwa 15:1
2Sa 22:3
Zb 3:3
Zb 84:11
o Zb 13:5
Zb 56:4
p Isa 61:10
q Kut 15:1
r 1Sa 16:13
2Sa 22:3
s Zb 20:6
Ebr 5:7
t Hes 23:20
Kum 9:29

Safu ya 2

a Kum 32:11
Zb 78:71
Isa 40:11

SURA 29

b 1Nya 16:28
Zb 96:7
Hab 3:3
c Zb 96:8
d 2Nya 20:21
e Zb 18:13
f Mdo 7:2
g 1Sa 7:10
Ayu 37:5
h Zb 93:4
Zb 104:3
i Ayu 26:11
Eze 10:5
j Ayu 40:9
k Isa 2:13
l Zb 114:4
Yer 4:24
m Kum 3:9
n Kut 19:18
Zb 77:18
Zb 144:5
Ebr 12:18
o Isa 13:13
Ebr 12:26
p Hes 13:26
q Ayu 39:1
r Isa 10:18
Eze 20:47
s Zb 48:9
Zb 63:2
Zb 134:1
Zb 135:2
t Mwa 6:17
Ayu 38:25

Na Yehova huketi akiwa
mfalme mpaka wakati
usio na kipimo.[a]
11 Yehova atawapa watu wake
nguvu kwelikweli.[b]
Yehova atawabariki kwa
amani watu wake.[c]

Muziki. Wimbo wa kuzindua nyumba.[d] Wa Daudi.

30 Nitakutukuza wewe,
Ee Yehova, kwa
maana umeniinua[e]
Nawe hukuwaruhusu adui
zangu washangilie juu
yangu.[f]
2 Ee Yehova Mungu wangu,
nilikulilia unisaidie,
nawe ukaniponya.[g]
3 Ee Yehova, umeitoa nafsi
yangu kutoka katika
Kaburi;*[h]
Umeendelea kuniweka
nikiwa hai, ili nisipate
kushuka ndani ya shimo.[i]
4 Mpigieni Yehova muziki,
enyi washikamanifu
wake,[j]
Utoleeni shukrani
ukumbusho wake
mtakatifu;[k]
5 Kwa sababu kuwa chini ya
hasira yake ni kwa muda
kidogo tu,[l]
Kuwa chini ya nia yake
njema ni kwa muda wote
wa maisha.[m]
Huenda kilio kikakaa
wakati wa jioni,[n] lakini
asubuhi kuna vigelegele
vya shangwe.[o]
6 Mimi nimesema katika
starehe yangu:[p]
"Sitatikiswa kamwe."[q]
7 Ee Yehova,
umeusimamisha mlima
wangu katika nguvu
kwa nia yako njema.[r]
Uliuficha uso wako;
nikawa na wasiwasi.[a]
8 Niliendelea kukuita,
Ee Yehova;[b]
Nami niliendelea kumsihi
Yehova anipe kibali.[c]
9 Damu yangu ina faida gani
ninaposhuka
katika shimo?[d]
Je, mavumbi yatakusifu
wewe?[e] Je, yatasema
juu ya ukweli wako?[f]
10 Usikie, Ee Yehova, na
kunionyesha kibali.[g]
Ee Yehova, uwe msaidizi
wangu.[h]
11 Umenibadilishia
maombolezo yangu
yakawa kucheza dansi;[i]
Umefungua nguo yangu ya
gunia, nawe unaendelea
kunifunga shangwe,[j]
12 Ili utukufu wangu upate
kukupigia muziki wala
usinyamaze.[k]
Ee Yehova Mungu wangu,
nitakusifu mpaka wakati
usio na kipimo.[l]

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

31 Nimekukimbilia wewe,
Ee Yehova.[m]
Ee nisiaibike kamwe.[n]
Niokoe katika uadilifu
wako.[o]
2 Unitegee sikio lako.[p]
Unikomboe haraka.[q]
Uwe ngome yangu yenye
miamba,[r]
Nyumba yenye ngome ili
kuniokoa.[s]
3 Kwa maana wewe ni
mwamba wangu na
ngome yangu;[t]
Nawe utaniongoza na
kunielekeza[u] kwa ajili
ya jina lako.[v]

SURA 29
a Zb 10:16; 1Ti 1:17
b Zb 28:9; Isa 40:29
c Hes 6:26; Zb 72:7; Zb 147:14; Ro 15:33; 1Ko 1:3

SURA 30
d 2Sa 5:11
e Zb 28:9
f Zb 25:2; Zb 41:11
g Mwa 20:17; Kut 15:26; 2Fa 20:5; Zb 6:2; Zb 103:3
h Zb 16:10; Zb 86:13; Mdo 2:31
i Zb 28:1; Isa 38:17; Yon 2:6
j 1Nya 16:4; Zb 32:11; Zb 145:10
k Kut 3:15; Zb 97:12
l Isa 12:1; Isa 54:8; 2Ko 4:17
m Zb 63:3
n Zb 6:6
o Zb 126:5
p Ayu 29:18
q Zb 15:5; Zb 16:8
r 2Sa 5:12; Zb 89:17

Safu ya 2
a Ayu 34:29; Zb 10:1; Zb 143:7
b Zb 34:6; Zb 77:1
c Flp 4:6
d Zb 28:1
e Zb 6:5; Zb 88:11; Zb 115:17; Mhu 9:10
f Isa 38:18
g Zb 143:1
h Zb 28:7; Zb 54:4
i 2Sa 6:14; Mhu 3:4; Yer 31:4
j Isa 61:3
k Zb 16:9; Zb 57:8
l Zb 9:1

SURA 31
m Zb 18:2
n Zb 22:5; Isa 49:23; Ro 5:5; Ro 10:11
o Zb 143:1
p Zb 71:2; Zb 130:2
q Zb 40:17; Zb 70:1; Lu 18:8
r 2Sa 22:3; Zb 18:2; Zb 94:22
s Zb 71:3; t 2Sa 22:2; u Zb 23:3; v Zb 25:11; Yer 14:7.

Zb 30:3* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

4 Utanitoa katika wavu
ambao wameuficha kwa
ajili yangu,[a]
Kwa maana wewe ni
ngome yangu.[b]
5 Naikabidhi roho yangu
mkononi mwako.[c]
Umenikomboa,[d] Ee Yehova
Mungu wa ukweli.[e]
6 Nawachukia wale
wanaoonyesha kujali
sanamu zisizo na faida,
za ubatili;[f]
Lakini mimi, namtegemea
Yehova.[g]
7 Nitakuwa na shangwe
na kushangilia katika
fadhili zako zenye
upendo,[h]
Kwa kuwa umeona mateso
yangu;[i]
Umejua juu ya taabu za
nafsi yangu.[j]
8 Wala hujanitia mkononi
mwa adui.[k]
Umeisimamisha miguu
yangu mahali penye
nafasi tele.[l]
9 Unionyeshe kibali, Ee
Yehova, kwa maana niko
katika dhiki kali.[m]
Mambo yenye kukera
yamefanya jicho langu
liwe dhaifu,[n] naam, nafsi
yangu na tumbo langu.[o]
10 Kwa maana uhai wangu
umefikia mwisho kwa
huzuni,[p]
Na miaka yangu kwa
kuugua.[q]
Kwa sababu ya kosa
langu nguvu zangu
zimejikwaa,[r]
Na mifupa yangu imekuwa
dhaifu.[s]
11 Nimekuwa shutuma[t]
kwa wale wote
wanaonionyesha uadui,[u]

SURA 31

a Zb 25:15
Zb 91:3
Mt 6:13
b Met 18:10
c Lu 23:46
Mdo 7:59
d Zb 71:23
e Kum 32:4
Ebr 6:18
f Yer 10:8
Yon 2:8
1Ko 8:4
g Zb 25:2
h Zb 13:5
i Zb 9:13
j Zb 142:3
1Ko 8:3
Ga 4:9
k Kum 32:30
1Sa 17:46
l Zb 4:1
Zb 18:19
m Met 14:10
n Ayu 17:7
Zb 6:7
Zb 88:9
o Zb 6:2
Zb 22:14
p Zb 88:15
Met 15:13
q Zb 71:9
r Zb 106:43
s Zb 32:3
Zb 102:3
t Zb 22:6
Zb 42:10
Zb 102:8
Isa 53:4
Ro 15:3
1Pe 4:14
u Zb 6:7
Mt 10:22
Mt 24:9
Lu 21:17

Safu ya 2

a Ayu 19:13
Zb 38:11
b Zb 88:8
c Mt 26:56
2Ti 4:16
d Zb 88:5
e Ro 9:22
f Yer 20:10
Lu 23:2
g Zb 37:4
Yer 6:25
h Lu 22:2
Lu 23:1
i Mt 27:1
j Zb 56:4
k Zb 16:2
Zb 43:5
Yoh 20:17
l 2Sa 7:12
m Zb 142:6
n Hes 6:25
Zb 67:1
Zb 80:3
Ro 9:15
o Zb 6:4
p Zb 25:2
Zb 69:6
Isa 50:7
Mt 27:46
q Ne 4:4
Ne 6:16
Zb 6:10
Isa 41:11
Yer 20:11
r 1Sa 2:9
Zb 115:17
Mhu 9:5
s Zb 12:3
Zb 63:11

Na nimekuwa hivyo hata
zaidi kwa jirani zangu,[a]
Na kitu chenye kutia hofu
kwa rafiki zangu.[b]
Wakati wanaponiona nje,
wamenikimbia.[c]
12 Nimesahaulika kama mtu
ambaye amekufa na
ambaye hayumo moyoni;[d]
Nimekuwa kama chombo
kilichoharibika;[e]
13 Kwa maana nimeisikia
habari mbaya kutoka
kwa wengi,[f]
Pande zote kukiwa na
woga.[g]
Wanapoungana kama kitu
kimoja dhidi yangu,[h]
Wanapanga hila ili
kuiondoa nafsi yangu.[i]
14 Lakini mimi—
nimekutegemea wewe,
Ee Yehova.[j]
Nimesema: "Wewe ni
Mungu wangu."[k]
15 Nyakati zangu ziko katika
mkono wako.[l]
Unikomboe kutoka katika
mkono wa adui zangu na
kutoka kwa wale
wanaonifuatilia.[m]
16 Uufanye uso wako
umwangazie mtumishi
wako.[n]
Uniokoe katika fadhili
zako zenye upendo.[o]
17 Ee Yehova, nisiaibike, kwa
maana nimekuita wewe.[p]
Waovu na waaibike;[q]
Na wakae kimya katika
Kaburi.*[r]
18 Midomo inayosema uwongo
na ishindwe kusema,[s]
Inayosema mambo dhidi ya
mwadilifu,[t] bila kujizuia

t 2Nya 32:16; Mt 10:25; Mdo 25:7.

Zb 31:17* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

katika majivuno na
dharau.[a]
19 Jinsi ulivyo mwingi
wema wako,[b] ambao
umewawekea hazina
wale wanaokuogopa![c]
Ambao umewapa wale
wanaokukimbilia wewe,
Mbele ya wana wa
binadamu.[d]
20 Utawaficha katika mahali
pa siri pa uso wako[e]
Mbali na ukusanyikaji
pamoja wa watu.[f]
Utawaficha katika kibanda
chako mbali na
kugombana kwa ndimi.[g]
21 Yehova na abarikiwe,[h]
Kwa maana amenionyesha
fadhili zenye upendo za
ajabu[i] katika jiji lililo
katika mkazo.[j]
22 Mimi nilisema hivi
niliposhikwa na
wasiwasi:[k]
"Hakika nitaangamizwa
kutoka mbele za macho
yako."[l]
Bila shaka umeisikia
sauti ya kusihi kwangu
nilipokulilia unisaidie.[m]
23 Enyi washikamanifu wake
wote, mpendeni Yehova.[n]
Yehova anawalinda
waaminifu,[o]
Lakini anampa malipo tele
yeyote anayeonyesha
majivuno.[p]
24 Iweni hodari, nayo mioyo
yenu na iwe na nguvu,[q]
Ninyi nyote mnaomngojea
Yehova.[r]

Ya Daudi. Maskili.

32 Mwenye furaha ni mtu
ambaye amesamehewa
maasi yake, ambaye
dhambi yake
imefunikwa.[s]
2 Mwenye furaha ni
mtu ambaye Yehova
hamhesabii kosa,[a]
Na ambaye katika
roho yake hamna
udanganyifu.[b]
3 Nilipokaa kimya mifupa
yangu ilichakaa kwa
sababu ya kuugua
kwangu mchana kutwa.[c]
4 Kwa maana mkono wako
ulikuwa mzito juu yangu
mchana na usiku.[d]
Umajimaji wa uhai wangu
umenyauka kama wakati
wa joto kavu la kiangazi.[e]
Sela.
5 Mwishowe niliungama
dhambi yangu kwako,
wala sikufunika kosa
langu.[f]
Nilisema: "Nitaungama
makosa yangu kwa
Yehova."[g]
Nawe mwenyewe
ukanisamehe kosa la
dhambi zangu.[h] *Sela*.
6 Kwa sababu hiyo kila aliye
mshikamanifu atasali
kwako[i]
Katika wakati ule tu
ambao wewe unaweza
kupatikana.[j]
Nayo mafuriko ya maji
mengi hayatamgusa.[k]
7 Wewe ni mahali pangu
pa kujificha; utanilinda
kutokana na taabu.[l]
Utanizingira kwa vigelegele
vya shangwe kwa sababu
ya kuniokoa.[m] *Sela*.
8 "Nitakufanya uwe
na ufahamu na
kukufundisha katika
njia unayopaswa
kuiendea.[n]

SURA 31

a Zb 94:4
b Zb 73:1
Isa 63:7
c Isa 64:4
1Ko 2:9
d Zb 126:2
Isa 26:12
e Zb 27:5
Zb 32:7
Mdo 3:19
f Zb 86:14
g Zb 64:3
h Ru 4:14
1Sa 25:39
Zb 68:19
Lu 1:68
i Zb 17:7
j 1Sa 23:7
k 1Sa 23:26
l Zb 88:16
Omb 3:54
Yon 2:4
m 2Nya 33:13
Zb 6:9
Met 15:29
Ebr 5:7
n Kum 10:12
Kum 30:20
Zb 34:9
o 1Sa 2:9
Zb 145:20
p 2Sa 22:28
Ayu 40:11
Zb 94:2
Isa 2:11
Yak 4:6
1Pe 5:5
q Zb 27:14
Isa 35:4
r Mwa 49:18
Zb 62:1
Zb 71:14
Omb 3:21
Mik 7:7
Tit 2:13

SURA 32

s Zb 85:2
Isa 1:18
Mdo 3:19
Ro 4:7

Safu ya 2

a Law 17:4
Ro 5:13
2Ko 5:19
b Yoh 1:47
c Met 28:13
d Zb 38:2
e Ayu 30:30
Zb 63:1
Zb 102:3
f Zb 38:18
Zb 51:4
1Yo 1:9
g Law 5:5
2Sa 12:13
2Nya 30:22
Zb 38:18
Zb 41:4
Mt 3:6
h Zb 86:5
Zb 103:3
Isa 44:22
Ho 14:2
Lu 7:47
i Zb 65:2
2Ko 1:3
j Zb 69:13
Isa 55:6
k Zb 124:4
Ufu 12:16
l Zb 9:9
Zb 27:5
Zb 119:114

m Kut 15:1; Amu 5:1; 2Sa 22:1; n Zb 27:11; Zb 86:11; Yer 7:23.

Nitakupa shauri
jicho langu likiwa
linakutazama.[a]
9 Msijifanye kama farasi
au nyumbu wasio na
uelewaji,[b]
Ambao roho yao yenye
nguvu huzuiwa na
hatamu au lijamu[c]
Kabla wao
hawajakukaribia wewe."[d]
10 Mwovu ana maumivu
mengi;[e]
Lakini mtu
anayemtegemea Yehova,
fadhili zenye upendo
humzingira.[f]
11 Shangilieni katika Yehova
na kuwa na shangwe,
enyi waadilifu;[g]
Na mpige vigelegele vya
shangwe, ninyi nyote
mlio wanyoofu katika
moyo.[h]

33 Pigeni vigelegele
vya shangwe, enyi
waadilifu, kwa sababu
ya Yehova.[i]
Sifa ni jambo linalofaa kwa
wanyoofu.[j]
2 Mtoleeni Yehova shukrani
kwa kinubi;[k]
Mpigieni muziki kwa
kinanda[l] chenye nyuzi
kumi.
3 Mwimbieni wimbo mpya;[m]
Fanyeni yote mnayoweza
katika kumpigia vinanda
pamoja na vigelegele vya
shangwe.[n]
4 Kwa maana neno la Yehova
ni la unyoofu,[o]
Nayo kazi yake yote ni kwa
uaminifu.[p]
5 Anapenda uadilifu na
haki.[q]
Dunia imejawa na fadhili
zenye upendo za Yehova.[r]

SURA 32

a Met 3:6
b Ayu 35:11
Met 26:3
Yer 8:6
c Yer 31:18
Yak 3:3
d Ayu 35:11
e Met 13:21
Ro 2:9
f Zb 34:8
Met 16:20
Yer 17:7
g Zb 68:3
Flp 4:4
h Zb 64:10

SURA 33

i Zb 32:11
Zb 97:12
Flp 4:4
j Zb 147:1
k Zb 81:2
l Zb 92:3
Zb 144:9
m Zb 40:3
Zb 98:1
Zb 149:1
Isa 42:10
Ufu 5:9
n 1Nya 13:8
Efe 5:19
o Zb 12:6
Met 30:5
p Zb 111:7
q Ayu 37:23
Zb 11:7
Zb 45:7
r Zb 145:16
Mdo 14:17

Safu ya 2

a Ebr 11:3
2Pe 3:5
b Mwa 2:1
Zb 104:30
c Mwa 1:9
Ayu 26:10
Ayu 38:8
Met 8:29
Yer 5:22
d Ufu 14:7
e Zb 76:7
f Mwa 1:3
Zb 148:5
g Zb 119:90
h Isa 8:10
Isa 19:3
i Zb 21:11
Zb 140:8
j Ayu 23:13
Met 19:21
Isa 46:10
k Zb 92:5
Isa 55:8
Yer 29:11
l Kum 33:29
Zb 144:15
m Zb 65:4
Zb 135:4
1Pe 2:9
n Zb 11:4
Zb 14:2
Met 15:3
o Ebr 4:13
p 1Fa 8:30
Zb 115:3
q 1Nya 28:9
Zb 105:25
r Ayu 34:21
Met 24:12

6 Mbingu zilifanywa kwa
neno la Yehova,[a]
Nayo majeshi yake yote
yalifanywa kwa roho ya
kinywa chake.[b]
7 Anayakusanya maji ya
bahari kana kwamba ni
kwa bwawa,[c]
Akiweka katika maghala
maji yenye kututumuka.
8 Wale wote walio wa dunia
na wamwogope Yehova.[d]
Wote wanaokaa katika
nchi yenye kuzaa na
wamhofu.[e]
9 Kwa maana yeye
mwenyewe alisema, na
ikawa hivyo;[f]
Yeye mwenyewe alitoa
amri, nayo ikasimama
hivyo.[g]
10 Yehova mwenyewe
amevunja shauri la
mataifa;[h]
Amezuia fikira za vikundi
vya watu.[i]
11 Shauri la Yehova
litasimama milele;[j]
Mawazo ya moyo wake ni
kwa kizazi kimoja baada
ya kizazi kingine.[k]
12 Lenye furaha ni taifa
ambalo Mungu wake ni
Yehova,[l]
Watu ambao amewachagua
wawe urithi wake.[m]
13 Kutoka mbinguni Yehova
ametazama,[n]
Amewaona wana wote wa
binadamu.[o]
14 Kutoka katika mahali
palipofanywa imara
ambako yeye hukaa[p]
Amewakazia macho wale
wote wanaokaa duniani.
15 Anaifanyiza mioyo
yao wote pamoja;[q]
Anazifikiria kazi zao zote.[r]

16 Hakuna mfalme
anayeokolewa kwa wingi
wa majeshi yake;[a]
Mtu mwenye nguvu
haokolewi kwa wingi wa
nguvu.[b]
17 Farasi ni udanganyifu kwa
ajili ya wokovu,[c]
Na kwa wingi wa nguvu
zake haokoi.[d]
18 Tazama! Jicho la Yehova
linawaelekea wale
wanaomwogopa,[e]
Wale wanaozingojea
fadhili zake zenye
upendo,[f]
19 Ili kuikomboa nafsi yao na
kifo,[g]
Na kuwahifadhi hai wakati
wa njaa.[h]
20 Nafsi yetu imekuwa
ikimtarajia Yehova.[i]
Yeye ni msaidizi wetu na
ngao yetu.[j]
21 Kwa maana moyo wetu
hushangilia katika yeye;[k]
Kwa maana tumelitegemea
jina lake takatifu.[l]
22 Fadhili zako zenye upendo,
Ee Yehova, na ziwe juu
yetu,[m]
Kwa vile tumeendelea
kukungojea.[n]

Ya Daudi, alipokuwa akijifanya mwenda-wazimu[o] mbele ya Abimeleki, hivi kwamba akamfukuza, naye akaenda zake.

א [*'A'leph*]

34 Nitambariki Yehova
nyakati zote;[p]
Daima sifa yake itakuwa
katika kinywa changu.[q]

ב [*Behth*]

2 Nafsi yangu itajisifu katika
Yehova;[r]
Wapole watasikia na
kushangilia.[s]

ג [*Gi'mel*]

3 Mtukuzeni Yehova pamoja
nami,[a]
Na tulikweze jina lake
pamoja.[b]

ד [*Da'leth*]

4 Nilimuuliza Yehova, naye
akanijibu,[c]
Naye akanikomboa kutoka
katika mambo yote
yenye kuniogopesha.[d]

ה [*He'*]

5 Walimtazama, wakang'aa,[e]
Nazo nyuso zao
hazingeweza kuona haya
kamwe.[f]

ז [*Za'yin*]

6 Huyu mwenye kuteseka
aliita, na Yehova
mwenyewe akasikia.[g]
Na Yeye akamwokoa
kutoka katika taabu
zake zote.[h]

ח [*Chehth*]

7 Malaika wa Yehova anapiga
kambi pande zote
kuwazunguka
wanaomwogopa,[i]
Na yeye huwaokoa.[j]

ט [*Tehth*]

8 Onjeni mwone ya kuwa
Yehova ni mwema;[k]
Mwenye furaha ni
mwanamume ambaye
humkimbilia.[l]

י [*Yohdh*]

9 Mwogopeni Yehova, enyi
watakatifu wake,[m]
Kwa maana wale
wanaomwogopa
hawakosi chochote.[n]

כ [*Kaph*]

10 Wana-simba wenye
manyoya shingoni
wamekuwa na vichache
na kukaa njaa;[o]

SURA 33

a Yos 11:6
2Nya 32:21
b Zb 44:5
Yer 9:23
c Kum 17:16
2Fa 7:7
Zb 20:7
Met 21:31
Isa 31:1
Ho 14:3
d Zb 147:10
e Ayu 36:7
Zb 34:15
1Pe 3:12
f Zb 147:11
g Zb 56:13
h Zb 37:19
Isa 33:16
i Zb 62:1
Zb 130:6
j Mwa 15:1
Kum 33:29
Zb 18:2
Zb 115:9
k Zb 13:5
Zek 10:7
l 1Nya 16:10
Zb 28:7
Met 18:10
m Zb 32:10
Zb 119:76
n Zb 31:24
Mik 7:7

SURA 34

o 1Sa 21:13
p Mdo 16:25
Efe 5:20
q Zb 44:8
Zb 71:8
r Isa 45:25
Yer 9:24
1Ko 1:31
s Zb 119:74

Safu ya 2

a Zb 35:27
Zb 69:30
Lu 1:46
b Zb 148:13
c Lu 11:9
Ebr 5:7
d Zb 18:48
Zb 144:10
e 2Ko 3:18
f Zb 37:19
g Zb 3:4
Zb 10:17
h 2Sa 22:1
i 2Fa 6:17
Zb 91:11
Mt 18:10
Mdo 5:19
Mdo 12:11
Ebr 1:14
j 2Fa 19:35
Da 6:22
k Yer 31:14
1Pe 2:3
l Zb 84:12
Zb 94:22
m Mwa 22:12
Zb 19:9
Ho 3:5
n Zb 23:1
Flp 4:19
o Ayu 4:11

Lakini kwa wale
wanaomtafuta Yehova,
hawatakosa chochote
chema.[a]

ל [*La′medh*]

11 Njooni, enyi wana,
nisikilizeni;[b]
Nitawafundisha
kumwogopa Yehova.[c]

מ [*Mem*]

12 Ni nani mtu yule
anayependezwa na uhai,[d]
Ambaye anapenda siku
za kutosha ili kuona
mema?[e]

נ [*Nun*]

13 Linda ulimi wako na yaliyo
mabaya,[f]
Na midomo yako isiseme
udanganyifu.[g]

ס [*Sa′mekh*]

14 Geuka kutoka katika
yaliyo mabaya, na
kufanya yaliyo mema;[h]
Utafute amani, na
kuifuatia.[i]

ע [*′A′yin*]

15 Macho ya Yehova
yanawaelekea waadilifu,[j]
Na masikio yake
yanakielekea kilio chao
cha kuomba msaada.[k]

פ [*Pe′*]

16 Uso wa Yehova uko dhidi ya
wale wanaotenda yaliyo
mabaya,[l]
Ili kumbukumbu lao
liondolewe mbali
duniani.[m]

צ [*Tsa·dheh′*]

17 Wao walilia kwa sauti,
naye Yehova mwenyewe
akasikia,[n]
Naye akawakomboa
kutoka katika taabu zao
zote.[o]

SURA 34

a Zb 23:6; Zb 84:11; Lu 1:53
b Met 4:1
c Ayu 28:28; Zb 111:10; Met 1:7; Met 8:13
d Kum 6:2; Kum 30:20; Zb 21:4; Zb 91:16; Mt 7:14; 1Pe 3:10
e Zb 4:6; Mhu 2:3
f Zb 39:1; Met 15:4; Yak 1:26; Yak 3:8
g Met 12:19; Met 12:22; Kol 3:9; 1Pe 2:1
h Zb 37:27; Zb 97:10; Met 3:7; Isa 1:16; Amo 5:15; Ro 12:9
i Mt 5:9; Ro 12:18; Ebr 12:14; 1Pe 3:11
j Ayu 36:7; Zb 33:18; 1Pe 3:12
k Zb 10:17; Zb 18:6; Zb 94:9; Isa 59:1
l Law 17:10; Yer 44:11; Eze 14:8; Amo 9:4
m Zb 10:16; Zb 37:10; Met 10:7; Isa 26:14
n Zb 30:2; Zb 91:15; Zb 145:18
o 2Nya 32:22; Zb 91:15; Mdo 12:11

Safu ya 2

a Zb 147:3; Isa 61:1
b Zb 51:17; Isa 57:15; Isa 66:2; Lu 4:18
c Met 24:16; Mdo 14:22; 2Ti 3:12
d Da 6:22; 1Ko 10:13
e Yoh 19:36
f Zb 94:23; Isa 3:11
g Zb 89:23; Yoh 7:7
h 1Fa 1:29; Zb 71:23; Zb 103:4; Omb 3:58
i Zb 9:10; Zb 84:11

SURA 35

j 1Sa 24:15; Zb 43:1; Zb 119:154

ק [*Qohph*]

18 Yehova yuko karibu na
wale waliovunjika moyo;[a]
Naye huwaokoa wale
waliopondwa roho.[b]

ר [*Rehsh*]

19 Mwadilifu ana misiba
mingi,[c]
Lakini Yehova humkomboa
kutoka katika yote hiyo.[d]

ש [*Shin*]

20 Yeye anailinda mifupa
yote ya mtu huyo;
Hakuna hata mmoja
uliovunjwa.[e]

ת [*Taw*]

21 Msiba utamuua mwovu;[f]
Na wale wanaomchukia
mwadilifu watahesabiwa
kuwa na hatia.[g]

22 Yehova anaikomboa nafsi
ya watumishi wake;[h]
Wala hakuna yeyote kati
ya wale wanaomkimbilia
atakayehesabiwa kuwa
na hatia.[i]

Ya Daudi.

35 Endesha kesi yangu
dhidi ya wapinzani
wangu, Ee Yehova;[j]
Upigane na wale
wanaopigana nami.[k]

2 Ushike ngao ndogo na
ngao kubwa,[l]
Na usimame ili unisaidie.[m]

3 Na uchomoe mkuki na
shoka lenye makali
kuwili ili kukutana na
wale wanaonifuatilia.[n]
Uiambie nafsi yangu:
“Mimi ni wokovu wako.”[o]

4 Wale wanaoiwinda nafsi
yangu na waone aibu na
kufedheheka.[p]

k Kut 14:25; Yos 10:42; Zb 3:7; l Kut 15:3; m Zb 33:20; Isa 42:13; n 1Sa 23:26; o Zb 62:7; Isa 12:2; p Zb 40:14; Zb 70:2; Yer 17:18.

Wale wanaonipangia hila
nipatwe na msiba na
warudishwe nyuma na
kufedheheka.[a]
5 Na wawe kama makapi
mbele ya upepo,[b]
Naye malaika wa Yehova
na awe akiwasukuma.[c]
6 Njia yao na iwe giza na
mahali penye kuteleza,[d]
Naye malaika wa Yehova
na awe akiwafuatilia.
7 Kwa maana wamenifichia
bila sababu shimo lao
lenye wavu;[e]
Wamelichimba bila sababu
kwa ajili ya nafsi yangu.[f]
8 Uharibifu na umjie bila
yeye kujua,[g]
Na wavu wake mwenyewe
aliouficha na umkamate;[h]
Na aanguke ndani yake
apatwe na uharibifu.[i]
9 Lakini nafsi yangu
mwenyewe na iwe na
shangwe katika Yehova;[j]
Na ishangilie katika
wokovu wake.[k]
10 Mifupa yangu yote na
iseme:[l]
"Ee Yehova, ni nani aliye
kama wewe,[m]
Anayemkomboa mwenye
kuteseka kutoka kwa
mwenye nguvu kuliko
yeye,[n]
Na kumkomboa mwenye
kuteseka na maskini
kutoka kwa mwenye
kumnyang'anya?"[o]
11 Mashahidi wenye jeuri
husimama;[p]
Huniuliza mambo
nisiyojua.[q]
12 Hunilipa mema yangu
kwa mabaya,[r]
Hasara kwa nafsi yangu.[s]
13 Lakini mimi, walipokuwa
wagonjwa, mavazi yangu
yalikuwa ni magunia,[a]
Nikaitesa nafsi yangu kwa
kufunga,[b]
Nayo sala yangu
mwenyewe ikawa ikirudi
kifuani pangu.[c]
14 Kana kwamba ni kwa
ajili ya mwenzangu, kana
kwamba ni kwa ajili ya
ndugu yangu,[d]
Nilitembea huku na
huku kama mtu
anayemwombolezea
mama yake.[e]
Nikainama nikiwa na
huzuni.
15 Lakini walishangilia na
kukusanyika pamoja
kuhusu kuchechemea
kwangu;[f]
Walikusanyika pamoja
dhidi yangu,[g]
Wakinipiga na
kuniangusha wakati
sikujua;[h]
Walinirarua
vipande-vipande wala
hawakukaa kimya.[i]
16 Kati ya wenye dhihaka,
walioasi imani, kwa
ajili ya keki,[j]
Kulikuwako kusaga meno
yao dhidi yangu.[k]
17 Ee Yehova, utaendelea
kuona hayo mpaka
wakati gani?[l]
Uirudishe nafsi yangu
kutoka katika
maangamizi yao,[m]
Naam, yangu iliyo ya
pekee[n] kutoka kwa
wana-simba wenye
manyoya shingoni.
18 Nitakusifu katika
kutaniko kubwa;[o]
Nitakusifu kati ya kikundi
cha watu wengi.[p]

SURA 35

a Zb 35:26
b Zb 1:4
Isa 17:13
Ho 13:3
Mt 3:12
c Kut 14:19
Isa 37:36
Mdo 12:23
d Zb 73:18
Met 4:19
Yer 23:12
e Zb 140:5
f Zb 119:85
g Met 29:1
h Zb 7:15
Zb 9:15
Zb 57:6
Zb 141:10
i Est 7:10
Zb 69:22
Ro 11:9
j 1Sa 2:1
Hab 3:18
k Zb 13:5
Zb 21:1
l Zb 22:14
m Kut 15:11
Zb 71:19
n Zb 18:17
Zb 37:40
o Zb 40:17
Met 22:23
p Zb 27:12
Mt 26:59
q Mdo 6:13
r 1Sa 19:5
Zb 38:20
Zb 109:5
Yer 18:20
Yoh 10:32
Yoh 18:23
s 1Sa 20:33

Safu ya 2

a Ayu 30:25
Zb 69:11
b Law 16:31
1Fa 21:27
Isa 58:3
c Lu 10:6
d 2Sa 1:17
e Mwa 24:67
f Met 17:5
g Zb 71:10
h Mt 27:30
i Mt 27:29
j Yoh 18:28
k Ayu 16:9
Zb 37:12
Mdo 7:54
l Hab 1:13
m Zb 69:14
Zb 142:6
n Zb 22:20
Zb 57:4
o Zb 22:22
Zb 40:9
Zb 111:1
Ebr 2:12
p Ro 15:9

19 Wale ambao ni adui zangu
bila sababu yoyote
wasishangilie juu yangu;[a]
Nao wale wanaonichukia
bila sababu, wasikonyeze
jicho.[b]
20 Kwa maana hawasemi
mambo ya amani;[c]
Bali juu ya wanyamavu
wa dunia
Wanaendelea kupanga
mambo ya udanganyifu.[d]
21 Nao hufungua kinywa chao
wazi dhidi yangu.[e]
Wamesema: "Aha! Aha!
jicho letu limeyaona."[f]
22 Ee Yehova, umeona.[g]
Usikae kimya.[h]
Ee Yehova, usikae mbali
nami.[i]
23 Uamke na ukae macho kwa
ajili ya hukumu yangu,[j]
Kwa ajili ya kesi yangu,[k]
Ee Mungu wangu, naam,
Yehova.
24 Nihukumu kulingana na
uadilifu wako, Ee Yehova
Mungu wangu,[l]
Nao wasishangilie juu
yangu.[m]
25 Na wasiseme moyoni
mwao: "Aha, nafsi
yetu!"[n]
Na wasiseme:
"Tumemmeza."[o]
26 Na waone aibu na
kufedheheka wote
pamoja[p]
Wanaoshangilia msiba
wangu.[q]
Na wavikwe aibu[r]
na fedheha wale
wanaojivuna sana
dhidi yangu.[s]
27 Wale wanaopendezwa
na uadilifu wangu na
wapige vigelegele kwa
shangwe na kushangilia.[t]
Nao waseme daima:[a]
"Yehova na atukuzwe,
ambaye anapendezwa
na amani ya mtumishi
wake."[b]
28 Nao ulimi wangu
mwenyewe na utamke
uadilifu wako kwa sauti
ya chini,[c]
Sifa yako mchana kutwa.[d]

Kwa kiongozi. Ya mtumishi wa Yehova, Daudi.

36 Maneno ya ukosaji kwa
mtu mwovu yako
katikati ya moyo
wake;[e]
Hakuna hofu ya Mungu
mbele ya macho yake.[f]
2 Kwa maana ametenda kwa
ulaini machoni pake
mwenyewe[g]
Asiweze kuliona kosa lake
ili alichukie.[h]
3 Maneno ya kinywa
chake ni kuumiza na
udanganyifu;[i]
Ameacha kuwa na
ufahamu wa kufanya
mema.[j]
4 Yeye anaendelea kupanga
hila ya kuumiza
kitandani mwake.[k]
Husimama katika njia
isiyo nzuri.[l]
Hakatai lililo baya.[m]
5 Ee Yehova, fadhili zako
zenye upendo ziko
mbinguni;[n]
Uaminifu wako umefika
mawinguni.[o]
6 Uadilifu wako ni kama
milima ya Mungu;[p]
Uamuzi wako wa hukumu
ni kilindi kikubwa cha
maji.[q]
Wewe huokoa mwanadamu
na mnyama, Ee Yehova.[r]

SURA 35

a Zb 25:2
b Zb 69:4; Met 6:13; Yoh 15:25
c Mt 26:4
d Zb 31:13; Yer 11:19; Mt 12:24; 1Pe 2:22
e Zb 22:13
f Zb 70:3
g Kut 3:7; Mdo 7:34
h Zb 28:1; Zb 50:21; Zb 83:1
i Zb 10:1; Zb 71:12
j Zb 44:23
k Zb 119:154
l Zb 7:8; Zb 26:1; Zb 96:13; Isa 11:4
m Zb 13:4
n Zb 70:3
o Zb 27:12; Zb 41:2; Zb 56:1
p Zb 40:14
q Yoh 16:20
r Zb 132:18
s Zb 38:16
t Ro 12:15; 1Ko 12:26

Safu ya 2

a Zb 70:4
b Zb 84:11; Zb 149:4
c Zb 51:14
d Zb 71:24; Zb 145:2

SURA 36

e Met 6:18
f Mwa 20:11; Ro 3:18
g Kum 29:19; Zb 10:3
h Zb 97:10; Amo 5:15
i Zb 5:9; Zb 12:2
j Yer 4:22
k Met 4:16; Mik 2:1
l Isa 65:2
m Ro 1:32
n Zb 57:10; Zb 103:11
o Zb 89:2; Zb 108:4
p Zb 71:19
q Ro 11:33
r Zb 145:9; Zb 147:9; 1Ti 4:10

7 Jinsi zilivyo na thamani
fadhili zako zenye
upendo, Ee Mungu![a]
Nao wana wa binadamu
hupata kimbilio katika
kivuli cha mabawa yako.[b]
8 Wao hunywa na kushiba
vinono vya nyumba
yako;[c]
Nawe huwanywesha
kwenye mito ya raha
zako.[d]
9 Kwa maana kwako wewe
iko chemchemi ya
uzima;[e]
Kwa nuru inayotoka
kwako sisi tunaweza
kuona nuru.[f]
10 Endeleza fadhili zako
zenye upendo kwa wale
wanaokujua,[g]
Na uadilifu wako kwa
wale walio wanyoofu
moyoni.[h]
11 Mguu wa majivuno
usinijie;[i]
Nao mkono wa watu
waovu, usinifanye kuwa
mtu wa kutanga-tanga.[j]
12 Huko wanaotenda
mambo yenye kuumiza
wameanguka;[k]
Wamesukumwa chini
nao wameshindwa
kusimama.[l]

Ya Daudi.

א [*'A'leph*]

37 Usijionyeshe umewaka
hasira kwa sababu ya
watenda-maovu.[m]
Usiwaonee wivu wale
wanaofanya mambo
yasiyo ya uadilifu.[n]
2 Kwa maana watakauka
haraka kama majani,[o]
Nao watafifia kama majani
mapya ya kijani kibichi.[a]

ב [*Behth*]

3 Mtegemee Yehova na
ufanye mema;[b]
Ukae duniani, na utende
kwa uaminifu.[c]
4 Pia upate furaha tele
katika Yehova,[d]
Naye atakupa maombi
ya moyo wako.[e]

ג [*Gi'mel*]

5 Mkabidhi Yehova njia
yako,[f]
Na kumtegemea,[g] naye
mwenyewe atatenda.[h]
6 Naye atauleta uadilifu
wako kama nuru,[i]
Na haki yako kama
katikati ya mchana.[j]

ד [*Da'leth*]

7 Kaa kimya mbele za
Yehova[k]
Na kumngojea kwa
kutamani.[l]
Usijionyeshe umewaka
hasira kwa sababu
ya mtu yeyote
anayeifanikisha
njia yake,[m]
Kwa sababu ya mtu
anayetimiza mawazo
yake.[n]

ה [*He'*]

8 Acha hasira na uache
ghadhabu;[o]
Usijionyeshe umewaka
hasira ili tu kufanya
uovu.[p]
9 Kwa maana
watenda-maovu
watakatiliwa mbali,[q]
Bali wale wanaomtumaini
Yehova ndio
watakaoimiliki dunia.[r]

SURA 36

a Zb 31:19
Mik 7:18
b Ru 2:12
Zb 17:8
Zb 91:4
c Zb 65:4
Yer 31:14
Zek 9:17
d Zb 16:11
e Ayu 33:4
Yer 2:13
Mdo 17:28
Ufu 4:11
f Ayu 29:3
Zb 27:1
Zb 43:3
Isa 2:5
2Ko 4:6
Yak 1:17
1Pe 2:9
g Zb 103:17
Yer 22:16
h Zb 7:10
Zb 94:15
Zb 97:11
i Zb 10:2
j Zb 16:8
k Zb 58:10
2Th 1:8
l Zb 1:5
Yer 51:64

SURA 37

m Zb 37:7
Met 24:19
n Zb 73:3
Met 3:31
Met 23:17
o Zb 73:19
Zb 90:6
Zb 129:6

Safu ya 2

a Yak 1:10
1Pe 1:24
b Zb 4:5
Isa 1:17
Isa 50:10
Ebr 13:16
c Met 28:20
d Isa 58:14
e Zb 21:2
f Zb 55:22
Met 16:3
g Mt 6:33
Flp 4:6
1Pe 5:7
h Mhu 9:1
Omb 3:37
Yak 4:15
i Mik 7:9
j Mal 3:18
Mt 7:2
k Zb 62:1
Omb 3:26
l Zb 27:14
m Ayu 21:7
Zb 73:3
Yer 12:1
n Met 19:21
Isa 10:13
o Met 14:29
Met 16:32
Efe 4:26
p Lu 9:54
q Ayu 27:14
Zb 55:23
2Pe 2:9
r Zb 25:13
Zb 37:29
Isa 57:13
Isa 58:14
Mt 5:5

ו [*Waw*]

10 Na bado muda kidogo
tu, na mtu mwovu
hatakuwako tena;[a]
Nawe hakika utapaangalia
mahali pake, naye
hatakuwapo.[b]
11 Bali wapole wataimiliki
dunia,[c]
Nao watapata furaha yao
tele katika wingi wa
amani.[d]

ז [*Za'yin*]

12 Mwovu anampangia hila
mwadilifu,[e]
Naye anamsagia meno
yake.[f]
13 Yehova mwenyewe
atamcheka,[g]
Kwa maana hakika yeye
anaona kwamba siku
yake itakuja.[h]

ח [*Chehth*]

14 Waovu wamechomoa
upanga na kuupinda
upinde wao,[i]
Ili kumwangusha mwenye
kuteseka na maskini,[j]
Ili kuwachinja walio
wanyoofu katika njia
yao.[k]
15 Upanga wao wenyewe
utaingia katika moyo
wao,[l]
Nazo pinde zao
zitavunjwa.[m]

ט [*Tehth*]

16 Afadhali kidogo alicho
nacho mtu mwadilifu[n]
Kuliko wingi wa watu
wengi waovu.[o]
17 Kwa maana mikono ya
waovu itavunjwa,[p]
Bali Yehova atakuwa
anawategemeza watu
waadilifu.[q]

SURA 37

a Ayu 24:24
Ebr 10:37
1Pe 4:7
b 1Sa 25:39
Ayu 7:10
Zb 52:5
c Isa 45:18
Mt 5:5
Ufu 21:3
d Zb 72:7
Zb 119:165
Isa 26:3
Isa 48:18
Flp 4:7
e 1Sa 18:21
Mt 26:4
f Zb 35:16
g Zb 2:4
h 1Sa 26:10
Yer 50:27
Eze 21:25
i Zb 64:3
j Hab 1:13
k Mdo 7:52
Mdo 12:2
1Yo 3:12
l 2Sa 17:23
Est 7:10
Zb 7:15
Zb 35:8
m Zb 46:9
Zb 76:3
n Met 16:8
Met 30:9
1Ti 6:6
o Met 15:16
Mhu 2:26
p Ayu 38:15
Zb 10:15
q Zb 41:12
Yud 24

Safu ya 2

a Zb 1:6
2Ti 2:19
b Zb 16:11
1Yo 2:25
c Mhu 9:12
Amo 5:13
d Zb 33:19
e Zb 92:9
Met 10:7
2Pe 2:12
f Mwa 19:29
g Zb 102:3
h Kum 28:12
Met 22:7
i Kum 15:11
Ayu 31:16
Zb 112:9
Met 14:21
Met 19:17
Mhu 11:2
2Ti 1:16
j Zb 37:9
k Zb 119:21
Zek 5:4
l 1Sa 2:9
Met 16:9
m Met 11:20
Yer 9:24
n Zb 34:19
Zb 145:14
Met 24:16
o Zb 91:12
p Ayu 32:6
Zb 71:18

י [*Yohdh*]

18 Yehova anazijua siku za
watu wasio na kosa,[a]
Nao urithi wao wenyewe
utaendelea mpaka
wakati usio na kipimo.[b]
19 Hawataona aibu wakati
wa msiba,[c]
Na katika siku za njaa
watashiba.[d]

כ [*Kaph*]

20 Kwa maana waovu
wataangamia,[e]
Nao adui za Yehova
watakuwa kama
malisho bora;
Lazima wao waufikie
mwisho wao.[f] Katika
moshi lazima waufikie
mwisho wao.[g]

ל [*La'medh*]

21 Mwovu anakopa lakini
halipi,[h]
Lakini mwadilifu
anaonyesha kibali na
anatoa zawadi.[i]
22 Kwa maana wale
wanaobarikiwa naye
wataimiliki dunia,[j]
Lakini wale anaowalaani
watakatiliwa mbali.[k]

מ [*Mem*]

23 Hatua za mwanamume
zimetayarishwa na
Yehova,[l]
Na Yeye hupendezwa na
njia yake.[m]
24 Ijapokuwa huenda
akaanguka, yeye
hatatupwa chini,[n]
Kwa maana Yehova
anautegemeza mkono
wake.[o]

נ [*Nun*]

25 Nilikuwa kijana, pia
nimezeeka,[p]

Na bado sijamwona mtu
yeyote mwadilifu akiwa
ameachwa kabisa,[a]
Wala uzao wake ukitafuta
mkate.[b]
26 Anaonyesha kibali na
kukopesha mchana
kutwa,[c]
Na kwa hiyo wazao wake
watapata baraka.[d]

ס [*Sa´mekh*]

27 Geuka mbali kutoka kwa
mambo mabaya na
ufanye yaliyo mema,[e]
Na hivyo ukae mpaka
wakati usio na kipimo.[f]
28 Kwa maana Yehova ni
mpenda-haki,[g]
Naye hatawaacha
washikamanifu wake.[h]

ע [*A´yin*]

Hakika watalindwa mpaka
wakati usio na kipimo;[i]
Lakini wazao wa waovu,
hakika watakatiliwa
mbali.[j]
29 Waadilifu wenyewe
wataimiliki dunia,[k]
Nao watakaa milele juu
yake.[l]

פ [*Pe´*]

30 Kinywa cha mwadilifu
ndicho kinachotamka
hekima kwa sauti ya
chini,[m]
Na ulimi wake ndio
unaosema kwa njia ya
haki.[n]
31 Sheria ya Mungu wake imo
katika moyo wake;[o]
Hatua zake
hazitayumba-yumba.[p]

צ [*Tsa·dheh´*]

32 Mwovu anaendelea
kumwangalia mwadilifu[q]
Naye anatafuta kumuua.[r]

SURA 37

a Yos 1:5; Zb 94:14; Mt 6:33; Ebr 13:5
b Kum 24:19; Zb 25:13; Zb 112:2; Zb 145:15; Met 10:3; Met 13:22
c Kum 15:8; Zb 112:5
d Met 20:7
e Zb 34:14; Isa 1:17; 1Pe 3:11
f Met 16:17
g Ayu 37:23; Zb 11:7; Zb 33:5; Yer 9:24
h 1Sa 2:9; 2Sa 22:26; Met 2:8
i Zb 97:10
j Ayu 27:14; Zb 21:10; Met 2:22
k Kum 30:20; Zb 37:9; Met 2:21; Mt 5:5
l Isa 66:22; Mt 25:46; Ufu 21:3
m Yos 1:8; Zb 1:2
n Mt 12:35; Efe 4:29; Kol 4:6
o Kum 6:6; Zb 40:8; Ebr 8:10
p Zb 121:3
q Yer 20:10; Lu 6:7
r Zb 10:8; Lu 19:47; Mdo 9:24

Safu ya 2

a Zb 31:8; 2Ti 4:17; 2Pe 2:9
b Zb 109:31
c Zb 27:14; Met 4:26; Met 20:22
d Zb 37:22
e Zb 52:6; Zb 91:8
f Est 5:11
g Ayu 21:7
h Kut 15:10; Mdo 12:23
i Zb 37:10
j Ayu 1:1
k Ayu 42:12; Ayu 42:16; Met 28:10; Isa 32:18

33 Lakini Yehova
hatamwacha mkononi
mwa huyo,[a]
Naye hatamtangaza kuwa
mwovu
anapohukumiwa.[b]

ק [*Qohph*]

34 Mtumaini Yehova na
kuishika njia yake,[c]
Naye atakuinua uimiliki
dunia.[d]
Watu waovu
watakapokatiliwa mbali,
wewe utaona hilo.[e]

ר [*Rehsh*]

35 Nimemwona mwovu akiwa
mwonevu[f]
Na akijitandaza kama mti
wenye majani mengi
katika udongo wa asili.[g]
36 Na bado yeye akapitilia
mbali, naye hakuwepo;[h]
Nami nikaendelea
kumtafuta, wala
hakupatikana.[i]

ש [*Shin*]

37 Mwangalie mtu asiye na
lawama na uendelee
kumwangalia mnyoofu,[j]
Kwa maana wakati ujao
wa mtu huyo utakuwa
wenye amani.[k]
38 Lakini wakosaji hakika
wataangamizwa pamoja;[l]
Wakati ujao wa
watu waovu hakika
utakatiliwa mbali.[m]

ת [*Taw*]

39 Nao wokovu wa watu
waadilifu ni kutoka kwa
Yehova;[n]
Yeye ni ngome yao wakati
wa taabu.[o]

l Zb 1:4; Zb 9:17; Zb 52:5; Met 10:7; **m** 2Pe 2:9; **n** Zb 3:8; Isa 12:2; Yon 2:9; **o** Zb 9:9; Zb 46:1; Zb 91:15; Isa 33:2.

40 Na Yehova atawasaidia na kuwaokoa.[a]
Atawaponya kutoka kwa watu waovu na kuwaokoa,[b]
Kwa sababu wamemkimbilia yeye.[c]

Muziki wa Daudi, wa kukumbusha.

38 Ee Yehova, usinikaripie katika hasira yako,[d]
Wala usinirekebishe katika ghadhabu yako.[e]
2 Kwa maana mishale yako imepenya sana ndani yangu,[f]
Nao mkono wako umeshuka juu yangu.[g]
3 Hakuna mahali popote pazima katika mwili wangu kwa sababu ya shutuma yako.[h]
Hakuna amani katika mifupa yangu kwa sababu ya dhambi yangu.[i]
4 Kwa maana makosa yangu yamepita juu ya kichwa changu;[j]
Kama mzigo mzito, ni mazito sana kwangu.[k]
5 Vidonda vyangu vinanuka, vina usaha,
Kwa sababu ya upumbavu wangu.[l]
6 Nimeingiwa na wasiwasi, nimeinama kupita kiasi;[m]
Nimetembea huku na huku kwa huzuni mchana kutwa.[n]
7 Kwa maana viuno vyangu vimejaa moto,
Wala hakuna mahali popote pazima katika mwili wangu.[o]
8 Nimekufa ganzi na kupondwa kupita kiasi;
Nimenguruma kwa sababu ya kuugua kwa moyo wangu.[a]
9 Ee Yehova, tamaa yangu yote iko mbele zako,
Wala kuugua kwangu hakujafichwa mbele zako.[b]
10 Moyo wangu mwenyewe umepiga-piga kwa nguvu, nguvu zangu zimeniacha,
Na nuru ya macho yangu mwenyewe haiko pamoja nami.[c]
11 Nao wenye kunipenda na wenzangu wanaendelea kusimama mbali na pigo langu,[d]
Na rafiki zangu wamesimama mbali.[e]
12 Lakini wale wanaoitafuta nafsi yangu wanatega mitego,[f]
Na wale wanaotaka kuniletea msiba wamesema mabaya,[g]
Nao kwa sauti ya chini wanaendelea kusema udanganyifu mchana kutwa.[h]
13 Lakini mimi, kama kiziwi, nikawa siwasikilizi;[i]
Na kama mtu asiyeweza kusema, nikawa sifungui kinywa changu.[j]
14 Nami nikawa kama mtu ambaye hasikii,
Na kinywani mwangu hamkuwa na hoja zozote za kupinga.
15 Kwa maana nilikungojea wewe, Ee Yehova;[k]
Wewe mwenyewe ukanijibu, Ee Yehova Mungu wangu.[l]
16 Kwa maana nilisema: “Kama sivyo

SURA 37
a Isa 31:5; Isa 46:4; 1Ko 10:13
b Zb 17:13; Zb 40:17
c 1Nya 5:20; Zb 22:4; Da 3:17; Da 6:23

SURA 38
d Zb 6:1; Ebr 12:6
e Kum 9:19; Yer 10:24
f Ayu 6:4; Omb 3:12
g Ru 1:13; Zb 32:4
h Zb 102:10; Isa 1:6
i Zb 6:2; Zb 31:10; Zb 41:4; Zb 51:8
j Ezr 9:6; Zb 40:12
k Mt 11:28
l Met 20:30
m Zb 35:14
n Ayu 30:28; Zb 42:9
o Zb 38:3

Safu ya 2
a Ayu 3:24; Zb 22:1; Isa 59:11
b Ro 8:23
c Zb 6:7; Zb 88:9
d Ayu 19:13; Zb 31:11
e Lu 23:49
f Zb 64:5; Zb 119:110; Lu 20:20
g 2Sa 16:7; Zb 62:4
h Zb 35:20; Met 24:2
i 2Sa 16:11
j Zb 39:2; Zb 39:9; Amo 5:13; 1Pe 2:23
k 2Sa 16:12; Zb 39:7; Zb 123:2
l Zb 138:3

watashangilia kwa
sababu yangu;[a]
Mguu wangu uliposonga
kwa kuyumba-yumba,[b]
hakika walijivuna sana
dhidi yangu.”[c]
17 Kwa maana nilikuwa
tayari kuchechemea,[d]
Na maumivu yangu
yalikuwa mbele yangu
daima.[e]
18 Kwa maana nilisema juu ya
kosa langu mwenyewe;[f]
Nikaanza kuhangaikia
dhambi yangu.[g]
19 Na adui zangu walio hai
wakawa wenye nguvu,[h]
Na wale wenye kunichukia
bila sababu wakawa
wengi.[i]
20 Nao walikuwa wakinilipa
mema yangu kwa
mabaya;[j]
Wakaendelea kushindana
nami kwa sababu ya
kufuatilia kwangu
mambo yaliyo mema.[k]
21 Usiniache, Ee Yehova.
Ee Mungu wangu, usikae
mbali nami.[l]
22 Ufanye haraka unisaidie,[m]
Ee Yehova wokovu wangu.[n]

Kwa kiongozi wa Yeduthuni.[o]
Muziki wa Daudi.

39 Nilisema: “Nitalinda njia
zangu[p]
Ili nisiendelee kutenda
dhambi kwa ulimi
wangu.[q]
Nitaweka lijamu kama
mlinzi wa kinywa
changu mwenyewe,[r]
Maadamu mtu yeyote
mwovu yuko mbele
yangu.”[s]
2 Nikawa asiyeweza kusema
kwa kukaa kimya;[t]

SURA 38

a Zb 13:4
Zb 35:24
b Zb 94:18
c Zb 35:26
d Zb 35:15
Yer 20:10
e Zb 77:2
f Zb 32:5
g Zb 51:3
h Zb 25:19
i Zb 35:19
Zb 69:4
j 1Sa 25:21
Zb 35:12
Yer 18:20
k 1Pe 3:13
1Yo 3:12
l Zb 22:11
Zb 35:22
m Zb 40:13
n Zb 27:1
Zb 62:2
Isa 12:2

SURA 39

o 1Nya 16:41
1Nya 25:1
p 1Fa 2:4
Zb 34:13
Zb 119:9
Ebr 2:1
1Pe 2:23
q Ayu 2:10
Zb 12:4
Met 18:21
Yak 3:5
r Zb 141:3
Yak 1:26
Yak 3:2
s Kol 4:5
t Zb 38:13
Mt 27:12

Safu ya 2

a Mt 7:6
b Yer 20:9
c Ayu 14:13
d Zb 89:47
Zb 90:12
Zb 119:84
e Ayu 14:1
f Zb 90:9
Yak 4:14
g Zb 90:4
2Pe 3:8
h Zb 62:9
Zb 144:4
i Ro 8:20
j Lu 12:19
k Ayu 27:17
Zb 49:10
Met 13:22
Mhu 2:19
Mhu 4:8
Lu 12:20
l Zb 38:15
m Zb 25:11
Mik 7:19
n Zb 44:13
Yoe 2:17
o Law 10:3
Ayu 40:4
p Zb 38:13
q 2Sa 16:10
Da 4:35

Nikaendelea kulinyamazia
lililo jema,[a]
Na kuumia kwangu
kukatengwa.
3 Moyo wangu ukawa na
moto ndani yangu;[b]
Wakati wa kuugua kwangu
moto ukaendelea
kuwaka.
Nilisema kwa ulimi wangu:
4 “Ee Yehova, nijulishe
mwisho wangu,[c]
Na kipimo cha siku
zangu—ni kipimo gani,[d]
Ili nipate kujua kadiri
nilivyo wa muda mfupi.[e]
5 Tazama! Umezifanya siku
zangu kuwa chache tu;[f]
Na urefu wa maisha yangu
si kitu mbele zako.[g]
Kwa kweli kila mtu
wa udongo, ingawa
anasimama imara, si kitu
ila pumzi tu.[h] *Sela*.
6 Kwa kweli mtu hutembea
huku na huku kama
kivuli tu.[i]
Kwa kweli wana
msukosuko ambao ni
ubatili.[j]
Mmoja anarundika vitu
wala hajui ni nani
atakayevikusanya.[k]
7 Na sasa, nimetumainia
nini, Ee Yehova?
Matarajio yangu
yanakuelekea wewe.[l]
8 Unikomboe kutoka katika
makosa yangu yote.[m]
Usiniweke kama shutuma
ya mtu asiye na akili.[n]
9 Niliendelea kuwa
asiyeweza kusema;[o]
sikuweza kufungua
kinywa changu,[p]
Kwa maana wewe
mwenyewe ulichukua
hatua.[q]

10 Uniondolee pigo lako.[a]
Nimefikia mwisho kwa
sababu ya uadui wa
mkono wako.[b]
11 Umemrekebisha mtu kwa
makaripio dhidi ya kosa,[c]
Nawe unakula vitu vyake
vyenye kutamanika
kama nondo.[d]
Kwa kweli kila mtu wa
udongo ni pumzi tu.[e]
Sela.
12 Uisikie sala yangu,
Ee Yehova,
Na usikilize kilio changu
cha kutaka msaada.[f]
Usikae kimya machozi
yangu yanapotoka.[g]
Kwa maana, kwako, mimi
ni mkaaji mgeni tu,[h]
Mhamiaji kama vile
mababu zangu wote.[i]
13 Usinitazame, ili nipate
kung'aa[j]
Kabla sijaenda, nisiwepo."[k]

Kwa kiongozi. Ya Daudi, muziki.

40 Nilimtumainia Yehova
kwa bidii,[l]
Kwa hiyo akanitegea sikio
lake na kusikia kilio
changu cha kuomba
msaada.[m]
2 Yeye pia akaniinua kutoka
katika shimo lenye
kunguruma,[n]
Kutoka katika matope ya
nchi.[o]
Kisha yeye akainua miguu
yangu juu ya mwamba;[p]
Akazifanya imara hatua
zangu.[q]
3 Tena, akatia wimbo mpya
katika kinywa changu,
Sifa kwa Mungu wetu.[r]
Wengi wataona hilo na
kuogopa,[s]
Nao watamtegemea
Yehova.[t]
4 Mwenye furaha ni
mwanamume ambaye
amemfanya Yehova
kuwa tegemeo lake[a]
Na ambaye hakuelekeza
uso wake kwa watu
wakaidi,
Wala kwa wale
wanaogeukia uwongo.[b]
5 Wewe mwenyewe
umefanya mambo
mengi,[c]
Ee Yehova Mungu wangu,
naam, kazi zako za ajabu
na mawazo yako
kutuelekea;[d]
Hakuna wa kulinganishwa
nawe.[e]
Ikiwa ningetaka kueleza
na kusema juu yake,
Zimekuwa nyingi sana
kuliko vile ninavyoweza
kusimulia.[f]
6 Hukupendezwa na dhabihu
na toleo;[g]
Haya masikio yangu
uliyafungua.[h]
Hukutaka toleo la
kuteketezwa na toleo la
dhambi.[i]
7 Kwa hiyo, nilisema:
"Tazama nimekuja,[j]
Katika kitabu cha
kukunjwa imeandikwa
juu yangu.[k]
8 Ee Mungu wangu,
nimependezwa na
kufanya mapenzi yako,[l]
Na sheria yako imo ndani
yangu.[m]
9 Nimetangaza habari njema
ya uadilifu katika
kutaniko kubwa.[n]
Tazama! Siizuii midomo
yangu.[o]
Ee Yehova, wewe
mwenyewe unajua hivyo
vema.[p]

SURA 39

a Ayu 9:34
Ayu 13:21
b Zb 90:7
c Zb 90:8
d Ayu 13:28
Isa 50:9
Isa 51:8
Ho 5:12
e Zb 39:5
Zb 102:11
f Zb 28:1
g Ayu 16:20
h Law 25:23
1Nya 29:15
Zb 119:19
1Pe 1:17
1Pe 2:11
i Mwa 47:9
Ebr 11:13
j Ayu 10:20
Ayu 14:6
k Ayu 14:10

SURA 40

l Zb 27:14
Zb 37:7
m Zb 34:15
Zb 116:2
n Zb 18:16
o Zb 69:2
p Zb 27:5
q Zb 37:23
r Zb 33:3
Zb 98:1
Zb 113:1
s Zb 52:6
Zb 64:9
t Mdo 4:4

Safu ya 2

a Zb 34:8
Yer 17:7
b Zb 101:3
Isa 28:15
c Kut 15:11
Zb 136:4
d Zb 92:5
Ufu 15:3
e Zb 89:6
Isa 55:8
f Zb 71:15
Zb 139:18
g 1Sa 15:22
Zb 51:16
Isa 1:11
Ho 6:6
Mt 12:7
Ebr 10:5
h Isa 50:5
i Ebr 10:6
j Ebr 10:7
k Mwa 3:15
Kum 18:15
Lu 24:44
Mdo 10:43
1Ko 15:3
l Zb 112:1
Yoh 4:34
Ro 7:22
Ebr 10:9
m Zb 37:31
Met 3:1
Yer 31:33
2Ko 3:3
n Zb 22:22
Zb 35:18
o Zb 119:13
Ebr 13:15
p Zb 139:2

10 Uadilifu wako sikuufunika
moyoni mwangu.[a]
Nimetangaza uaminifu
wako na wokovu wako.[b]
Sikuficha fadhili zako
zenye upendo na ukweli
wako katika kutaniko
kubwa.”[c]
11 Wewe mwenyewe,
Ee Yehova, usinizuilie
huruma zako.[d]
Fadhili zako zenye upendo
na ukweli wako zinilinde
daima.[e]
12 Kwa maana misiba
ilinizunguka mpaka
ikawa haihesabiki.[f]
Makosa yangu mengi zaidi
yalinifikia kuliko vile
nilivyoweza kuona;[g]
Yakawa mengi sana
kuliko nywele za kichwa
changu,[h]
Nao moyo wangu
mwenyewe uliniacha.[i]
13 Ee Yehova, upendezwe na
kunikomboa.[j]
Ee Yehova, ufanye haraka
kuja kunisaidia.[k]
14 Na waone aibu
na kufedheheka wote
pamoja[l]
Wale wanaoitafuta nafsi
yangu wapate kuifagilia
mbali.[m]
Wale wanaopendezwa na
msiba wangu na wageuke
na kufedheheshwa.[n]
15 Na wakodoe macho kwa
mshangao kwa sababu ya
aibu yao[o]
Wale wanaoniambia: “Aha!
Aha!”[p]
16 Na hao washangilie na
kukufurahia wewe,[q]
Wale wote
wanaokutafuta.[r]
Na waseme daima: “Yehova
na atukuzwe,”[s]
Wale wanaopenda wokovu
wako.[a]
17 Lakini mimi ninateseka
nami ni maskini.[b]
Yehova mwenyewe
ananijali.[c]
Wewe ni msaidizi wangu
na Mwokoaji wangu.[d]
Ee Mungu wangu,
usichelewe mno.[e]

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi.

41 Mwenye furaha ni mtu
yeyote anayetenda
kwa kumfikiria mtu
wa hali ya chini;[f]
Katika siku ya msiba
Yehova atamwokoa.[g]
2 Yehova mwenyewe
atamlinda na
kumhifadhi hai.[h]
Atatangazwa kuwa
mwenye furaha duniani;[i]
Nawe huwezi kamwe
kumtia mkononi mwa
nafsi ya adui zake.[j]
3 Yehova mwenyewe
atamtegemeza katika
kitanda cha ugonjwa;[k]
Kitanda chake chote
hakika utakibadilisha
wakati wa ugonjwa
wake.[l]
4 Mimi nami, nilisema:
“Ee Yehova, nionyeshe
kibali.[m]
Uiponye nafsi yangu, kwa
maana nimekutendea
dhambi.”[n]
5 Nao adui zangu, wanasema
mabaya juu yangu:[o]
“Atakufa wakati gani na
jina lake kwa kweli
lipotee?”
6 Na mtu akija kuniona,
moyo wake utasema
mambo yasiyo ya kweli;[p]
Atajikusanyia jambo lenye
kuumiza;

SURA 40
a Mdo 20:27
b Ebr 2:13
c Ebr 2:12
d Zb 69:16
e Zb 43:3
Zb 57:3
Zb 61:7
f Zb 71:20
g Zb 38:4
h Zb 69:4
i Zb 73:26
j Zb 25:17
k Zb 38:22
Zb 50:15
Zb 70:1
l Zb 31:17
Zb 35:4
Zb 70:2
Zb 71:13
m Mt 21:38
n Zb 9:3
o Zb 70:3
Zb 73:19
p Zb 35:25
q Zb 13:5
Zb 68:3
r Kum 4:29
Zb 70:4
s Zb 35:27
Lu 1:46

Safu ya 2
a Zb 3:8
Zb 85:9
b Zb 70:5
c 1Pe 5:7
d Zb 54:4
Isa 50:7
Ebr 13:6
e Zb 143:7

SURA 41
f Kum 15:7
Zb 112:9
Met 14:21
Met 22:9
g Zb 37:39
h Zb 145:20
Yer 45:5
i Zb 128:1
Mt 5:7
Lu 1:48
j Zb 27:12
2Pe 2:9
k 2Fa 20:5
Zb 103:3
l Flp 2:27
m Zb 32:5
Zb 51:1
n Zb 6:2
Zb 38:3
Zb 147:3
Met 28:13
o Zb 102:8
p Zb 12:2
Met 26:24

Atatoka nje; huko nje
atalisema.[a]
7 Wote wanaonichukia
wananong'onezana
juu yangu kwa
muungano;[b]
Wanaendelea kupanga
hila ya jambo baya juu
yangu:[c]
8 "Jambo lisilofaa kitu
linamiminwa juu yake;[d]
Sasa kwa kuwa amelala
chini, hatasimama
tena."[e]
9 Pia mtu mwenye kuwa
na amani nami, ambaye
nimemtegemea,[f]
Ambaye alikuwa akila
mkate wangu,[g]
amekiinua kisigino
chake dhidi yangu.[h]

SURA 41

a Mt 26:61
b Met 16:28
Ro 1:29
2Ko 12:20
c Zb 31:13
Zb 56:5
d Zb 101:3
e Zb 3:2
Zb 71:11
f 2Sa 15:12
Ayu 19:19
Zb 55:13
g Oba 7
h Mk 14:18
Yoh 13:18
Yoh 13:26

Safu ya 2

a Zb 57:1
b Zb 18:37
c Zb 31:8
Zb 124:6
Yer 20:13
d Ayu 1:1
Zb 25:21
Met 2:7
Met 10:29
e Zb 34:15
Zb 140:13
f 1Nya 29:10
Lu 1:68
g 1Nya 16:36
Ufu 7:12
h Zb 72:19
1Ko 14:16

10 Wewe, Ee Yehova,
unionyeshe kibali na
kuniinua,[a]
Ili nipate kuwalipa.[b]
11 Kwa jambo hili ninajua
kwamba umependezwa
nami,
Kwa sababu adui yangu
hapigi kelele za ushindi
juu yangu.[c]
12 Nami, umenitegemeza kwa
sababu ya utimilifu wangu,[d]
Nawe utaniweka mbele
za uso wako mpaka
wakati usio na kipimo.[e]
13 Yehova Mungu wa Israeli
na abarikiwe[f]
Tangu wakati usio na
kipimo mpaka wakati
usio na kipimo.[g]
Amina na Amina.[h]

KITABU CHA PILI
(Zaburi 42 – 72)

Kwa kiongozi.
Maskili kwa ajili
ya wana wa Kora.[a]

42 Kama vile paa ambaye
hutamani vijito vya
maji,
Ndivyo nafsi yangu
inavyokutamani wewe,
Ee Mungu.[b]
2 Kwa kweli nafsi yangu ina
kiu kwa ajili ya Mungu,[c]
kwa ajili ya Mungu
aliye hai.[d]
Ni wakati gani
nitakapokuja nionekane
mbele za Mungu?[e]
3 Machozi yangu yamekuwa
chakula changu mchana
na usiku,[f]
Huku wakiniambia
mchana kutwa: "Mungu
wako yuko wapi?"[g]
4 Nitakumbuka mambo haya,
nami nitaimimina nafsi
yangu iliyo ndani yangu.[h]

SURA 42

a 1Nya 6:37
b Isa 26:8
c Zb 63:1
d Kum 32:40
Yos 3:10
Yer 10:10
Mt 16:16
1Th 1:9
e Zb 27:4
Zb 84:2
f Zb 80:5
Zb 102:9
g Zb 3:2
Zb 79:10
h Ayu 30:16
Zb 62:8

Safu ya 2

a 1Nya 16:1
b Kum 16:14
Efe 5:19
Kol 3:16
c Kum 16:16
2Nya 30:23
d Zb 55:4
Mk 14:34
e Zb 43:5
f Zb 37:7
Zb 71:14
Omb 3:24
Mik 7:7
g Zb 43:5
h Zb 22:1
Zb 43:5
Met 12:25
Yoh 12:27

Kwa maana nilikuwa
nikipita pamoja na watu
wengi,
Nilikuwa nikitembea
polepole mbele yao
kwenda kwenye nyumba
ya Mungu,[a]
Kwa sauti ya vigelegele vya
shangwe na shukrani,[b]
Ya umati unaofanya
sherehe.[c]
5 Kwa nini umekata tamaa,
Ee nafsi yangu,[d]
Na kwa nini una
msukosuko ndani
yangu?[e]
Mngojee Mungu,[f]
Kwa maana bado nitamsifu
kuwa ndiye wokovu
wangu mkuu.[g]
6 Ee Mungu wangu, nafsi
yangu mwenyewe
imekata tamaa ndani
yangu.[h]

Ndiyo sababu
ninakukumbuka,[a]
Kutoka katika nchi ya
Yordani na vilele vya
Hermoni,[b]
Kutoka katika ule mlima
mdogo.[c]
7 Kilindi cha maji kinaita
kilindi cha maji
Kwa sauti ya mabubujiko
yako ya maji.
Mashuu yako yote na
mawimbi yako[d]—
Yamepita juu yangu.[e]
8 Wakati wa mchana Yehova
ataamuru fadhili zake
zenye upendo,[f]
Na wakati wa usiku wimbo
wake utakuwa nami;[g]
Kutakuwako sala kwa
Mungu wa uhai wangu.[h]
9 Nitamwambia Mungu
mwamba wangu:[i]
"Kwa nini umenisahau?[j]
Kwa nini natembea kwa
huzuni kwa sababu ya
ukandamizaji wa adui?"[k]
10 Wale wanaonionyesha
uadui wamenishutumu
kwa mauaji dhidi ya
mifupa yangu,[l]
Huku wakiniambia
mchana kutwa: "Mungu
wako yuko wapi?"[m]
11 Kwa nini umekata tamaa,
Ee nafsi yangu,[n]
Na kwa nini una
msukosuko ndani
yangu?[o]
Mngojee Mungu,[p]
Kwa maana bado nitamsifu
kuwa ndiye wokovu
wangu mkuu na kuwa
ndiye Mungu wangu.[q]

43 Unihukumu,[r] Ee Mungu,
Na uendeshe kesi[s] yangu
dhidi ya taifa lisilo
shikamanifu.

SURA 42
a Yon 2:7
b Kum 3:8
c Zb 48:2
Zb 68:16
Zb 132:13
d Zb 88:7
e Yon 2:3
f Kum 28:8
g Ayu 35:10
Zb 32:7
Zb 63:6
h Zb 27:1
i 2Sa 22:2
j Zb 13:1
k Zb 38:6
Zb 43:2
Mhu 4:1
l Zb 31:11
Zb 102:8
m Zb 3:2
Zb 79:10
Yoe 2:17
Mik 7:10
n Zb 42:5
o Zb 43:5
p Zb 37:7
Zb 71:14
q Zb 42:5

SURA 43
r Zb 7:8
Zb 26:1
Zb 35:24
s 1Sa 24:15
Zb 35:1
Met 22:23

Safu ya 2
a Zb 71:4
b Zb 28:7
Zb 140:7
c Zb 42:9
d Ayu 29:3
Zb 40:11
Met 6:23
e Zb 5:8
Zb 27:11
Zb 143:10
f 1Nya 16:1
Zb 3:4
Zb 78:68
g Zb 84:3
Ebr 13:10
h Isa 61:10
i 2Sa 6:5
Zb 81:2
j Zb 42:5
k Zb 37:7
Zb 71:14
l Zb 42:11

SURA 44
m 1Nya 6:37
n Kut 13:14
Amu 6:13
Zb 78:3
o Isa 38:19
p Hes 21:14
q Kum 7:1
Zb 78:55
Zb 105:44

Uniokoe kutoka kwa mtu
wa udanganyifu na
mwenye kukosa uadilifu.[a]
2 Kwa maana wewe ni
Mungu wa ngome yangu.[b]
Kwa nini umenitupilia
mbali?
Kwa nini natembea kwa
huzuni kwa sababu ya
ukandamizaji wa adui?[c]
3 Tuma nuru yako na kweli
yako.[d]
Na hivyo vyenyewe
viniongoze.[e]
Navyo vinilete kwenye
mlima wako mtakatifu na
kwenye maskani
yako kuu.[f]
4 Nami nitakuja kwenye
madhabahu ya Mungu,[g]
Kwa Mungu, ambaye
ni kushangilia kwangu
kwa furaha.[h]
Nami nitakusifu kwa
kinubi, Ee Mungu,
Mungu wangu.[i]
5 Kwa nini umekata tamaa,
Ee nafsi yangu,[j]
Na kwa nini una
msukosuko ndani yangu?
Mngojee Mungu,[k]
Kwa maana bado nitamsifu
kuwa ndiye wokovu
wangu mkuu na kuwa
ndiye Mungu wangu.[l]

Kwa kiongozi.
Ya wana wa Kora.[m] Maskili.

44 Ee Mungu, tumesikia
kwa masikio yetu,
Mababu zetu wenyewe
wametusimulia[n]
Utendaji ambao ulifanya
katika siku zao,[o]
Siku za zamani za kale.[p]
2 Wewe mwenyewe
kwa mkono wako
uliwafukuzia mbali
mataifa,[q]

Nawe ukawapanda hao
badala yao.[a]
Ukavunja vikundi vya
mataifa na kuwafukuza.[b]
3 Kwa maana hawakuimiliki
nchi hiyo kwa upanga
wao wenyewe,[c]
Wala wokovu haukuletwa
kwa mkono wao
wenyewe.[d]
Kwa maana ulikuwa ni
mkono wako wa kuume,[e]
naam, mkono wako na
nuru ya uso wako,
Kwa sababu ulipendezwa
nao.[f]
4 Wewe mwenyewe ni Mfalme
wangu, Ee Mungu.[g]
Amuru wokovu mkuu
kwa ajili ya Yakobo.[h]
5 Kupitia wewe
tutawasukuma
wapinzani wetu;[i]
Katika jina lako
tutawakanyagia chini
wale wanaosimama
dhidi yetu.[j]
6 Kwa maana sikuendelea
kuutegemea upinde
wangu[k]
Wala si upanga wangu
uliokuwa ukiniokoa.[l]
7 Kwa maana ulituokoa
kutoka kwa wapinzani
wetu,[m]
Nawe ukawafanya waone
aibu wale wanaotuchukia
vikali.[n]
8 Tutamtolea Mungu sifa
mchana kutwa,[o]
Nasi tutalisifu jina lako
mpaka wakati usio na
kipimo.[p] *Sela*.
9 Lakini sasa umetutupilia
mbali na unaendelea
kutufedhehesha,[q]
Wala huendi pamoja na
majeshi yetu.[r]

SURA 44
a Kut 15:17
Zb 80:8
b Yos 10:11
Yos 24:12
Zb 135:10
Zb 136:17
c Kum 4:38
Kum 8:17
d 1Sa 12:22
e Isa 63:12
f Kum 7:8
g Zb 24:10
Zb 74:12
Isa 33:22
h Zb 53:6
i Zb 18:39
Flp 4:13
j Zb 60:12
k Zb 20:7
Zb 33:16
l 1Sa 17:45
Ho 1:7
m Yos 24:8
n Zb 40:14
Zb 132:18
o Zb 34:2
p Zb 115:1
q Zb 43:2
Zb 74:1
r Zb 60:10

Safu ya 2
a Kum 28:25
Yos 7:8
1Sa 31:1
b Zb 89:41
Yer 15:13
c Zb 119:176
Ro 8:36
d Kum 28:64
e Kum 32:30
Isa 52:3
f Zb 79:4
Zb 80:6
g Zb 123:4
h Kum 28:37
2Nya 7:20
Yer 24:9
i Omb 2:15
j Yer 51:51
k Zb 8:2
l Kum 6:12
m Kut 34:10
n Ebr 3:12
o Ayu 23:11
Zb 119:157
p Isa 34:13
Isa 35:7

10 Wewe unaendelea
kutufanya tugeuke
kutoka kwa adui zetu,[a]
Na wale wanaotuchukia
vikali wamejinyakulia
vitu.[b]
11 Wewe unatutoa kama
kondoo, kama chakula,[c]
Nawe umetutawanya kati
ya mataifa.[d]
12 Unawauza watu wako kwa
bei ndogo sana,[e]
Wala hujapata faida yoyote
kwa bei yao.
13 Unatuweka kuwa shutuma
kwa jirani zetu,[f]
Kuwa dharau na dhihaka
kwa wale
wanaotuzunguka
pande zote.[g]
14 Umetufanya kuwa neno
la kimethali kati ya
mataifa,[h]
Kuwa kitu cha kutikisiwa
kichwa kati ya vikundi
vya mataifa.[i]
15 Fedheha yangu iko mbele
yangu mchana kutwa,
Nayo aibu ya uso wangu
mwenyewe imenifunika,[j]
16 Kwa sababu ya sauti ya
mtu anayeshutumu na
kusema vibaya,
Kwa sababu ya adui na mtu
anayejilipizia kisasi.[k]
17 Yote hayo ndiyo yametujia,
nasi hatujakusahau,[l]
Wala hatujatenda kwa njia
ya uwongo katika agano
lako.[m]
18 Moyo wetu haujageuka
nyuma kwa kukosa
imani,[n]
Wala hatua za miguu yetu
hazitoki katika njia yako.[o]
19 Kwa maana umetuponda
katika mahali pa
mbwa-mwitu,[p]

Nawe unatufunika kwa
kivuli kizito.[a]
20 Ikiwa tumelisahau jina la
Mungu wetu,
Au kumnyooshea mungu
mgeni mikono yetu,[b]
21 Je, Mungu mwenyewe
hatachunguza hilo?[c]
Kwa maana yeye anajua
siri za moyo.[d]
22 Lakini kwa ajili
yako tumeuawa mchana
kutwa;
Tumehesabiwa kuwa
kondoo wa kuchinjwa.[e]
23 Uamke. Kwa nini
unaendelea kulala
usingizi, Ee Yehova?[f]
Uamke. Usiendelee
kututupilia mbali milele.[g]
24 Kwa nini unaendelea
kuuficha uso wako?
Kwa nini unasahau mateso
yetu na ukandamizaji
wetu?[h]
25 Kwa maana nafsi
yetu imeinama chini
mavumbini;[i]
Tumbo letu limeshikamana
na udongo.
26 Usimame, utusaidie[j]
Na kutukomboa kwa ajili
ya fadhili zako zenye
upendo.[k]

Kwa kiongozi juu ya Mayungiyungi. Ya wana wa Kora. Maskili. Wimbo wa wanawake wapendwa.

45 Moyo wangu
umesisimuka kwa
sababu ya jambo jema.[l]
Ninasema: "Kazi zangu
zinamhusu mfalme."[m]
Ulimi wangu na uwe
kalamu[n] ya mwandikaji
stadi.[o]
2 Kwa kweli wewe una sura
nzuri kuliko wana wa
binadamu.[p]
Uvutio umemiminwa juu
ya midomo yako.[a]
Ndiyo sababu Mungu
amekubariki mpaka
wakati usio na kipimo.[b]
3 Funga upanga[c] wako
kwenye paja lako, ewe
mwenye nguvu,[d]
Pamoja na utukufu wako
na fahari yako.[e]
4 Na katika fahari yako
endelea mpaka
ufanikiwe;[f]
Panda kwa kutetea kweli
na unyenyekevu na
uadilifu,[g]
Na mkono wako wa kuume
utakufundisha mambo
yenye kuogopesha.[h]
5 Mishale yako ni mikali
—vikundi vya watu
vinaendelea kuanguka
chini yako[i]—
Katika moyo wa adui za
mfalme.[j]
6 Mungu ni kiti chako cha
ufalme mpaka wakati
usio na kipimo, naam,
milele;[k]
Fimbo ya enzi ya ufalme
wako ni fimbo ya
unyoofu.[l]
7 Umependa uadilifu[m] nawe
unachukia uovu.[n]
Ndiyo sababu Mungu,
Mungu wako,[o] amekutia
mafuta[p] kwa mafuta ya
kushangilia[q] kuliko
wenzako.[r]
8 Mavazi yako yote ni
manemane na udi na
kida;[s]
Kutoka katika jumba kuu
la mfalme la pembe,[t]
vinanda vimekufanya
ushangilie.
9 Binti[u] za wafalme wamo
kati ya wanawake wako
wenye thamani.

SURA 44
a Zb 23:4
b Kut 20:3
c Zb 139:1
Yer 17:10
d Mhu 12:14
e Zb 79:2
Ro 8:36
f Zb 7:6
Zb 78:65
g Ayu 13:24
Zb 13:1
Zb 88:14
h Isa 40:27
i Zb 119:25
Isa 51:23
j Zb 33:20
k Zb 26:11
Zb 130:7

SURA 45
l Zb 49:3
m Zb 2:6
1Pe 1:11
n 2Sa 23:2
Isa 8:1
Yer 8:8
o Ezr 7:6
p Wim 5:10

Safu ya 2
a Yoh 7:46
b Zb 72:17
c Ufu 1:16
Ufu 19:15
d Isa 9:6
e Ebr 1:3
f Ufu 6:2
g Ufu 19:11
h Ufu 6:15
i Zb 2:9
2Th 1:8
j Ufu 17:14
Ufu 19:19
k Zb 89:29
Zb 89:36
l Isa 11:4
Yer 33:15
Ebr 1:8
m Mt 3:15
Ebr 7:26
n Mt 7:23
Ebr 1:9
o Yoh 20:17
p Isa 61:1
Mdo 4:27
Mdo 10:38
q Zb 21:6
r 1Nya 29:23
2Nya 13:5
2Nya 13:8
Mt 1:6
s Wim 1:3
Wim 4:14
t 1Fa 22:39
u Isa 60:4

Malkia[a] amesimama
kwenye mkono wako wa
kuume akiwa amevaa
dhahabu ya Ofiri.[b]
10 Sikiliza, ewe binti, uone, na
utege sikio lako;
Na uwasahau watu wako na
nyumba ya baba yako.[c]
11 Naye mfalme atautamani
urembo wako,[d]
Kwa maana yeye ni bwana
wako,[e]
Kwa hiyo mwinamie.[f]
12 Binti Tiro na zawadi pia[g]—
Walio matajiri kati ya watu
watautuliza uso wako
mwenyewe.[h]
13 Binti ya mfalme ana
utukufu wote ndani ya
nyumba;[i]
Mavazi yake yamepambwa
kwa dhahabu.
14 Atapelekwa kwa mfalme
akiwa na mavazi
yaliyofumwa.[j]
Mabikira katika msafara
wake ambao ni rafiki
zake wanaingizwa ndani
kwako.[k]
15 Watapelekwa kwa furaha
na shangwe;
Wataingia katika jumba la
mfalme.
16 Mahali pa mababu[l] zako
patachukuliwa na wana
wako,[m]
Ambao utawaweka kuwa
wakuu katika dunia
yote.[n]
17 Nitalitaja jina lako
katika vizazi vyote
vitakavyokuja.[o]
Ndiyo sababu vikundi vya
watu vitakusifu mpaka
wakati usio na kipimo,
naam, milele.

SURA 45
a Ufu 19:7
b Isa 13:12
c Wim 2:10
Ufu 14:4
d Wim 1:8
Wim 2:2
e Efe 5:23
Yud 4
f 1Fa 1:16
Flp 2:10
g 2Sa 5:11
h Zb 72:10
Isa 49:23
i Ufu 19:7
j Ufu 19:8
Ufu 21:2
k Wim 2:7
Wim 5:9
Wim 6:1
l Mt 1:1
m Isa 9:6
n Isa 32:1
o Zb 72:17

Safu ya 2

SURA 46
a 1Nya 6:37
b Zb 62:7
Met 14:26
Isa 25:4
c Kum 4:7
Zb 145:18
Nah 1:7
d 2Pe 3:10
e Isa 54:10
f Zb 93:4
Yer 5:22
g Amu 5:5
Mik 1:4
Nah 1:5
h 2Nya 6:6
Zb 48:1
Isa 60:14
i Zb 43:3
j Kum 23:14
Zb 132:13
Isa 12:6
Ho 11:9
k Ebr 12:28
l Kut 14:24
Zb 30:5
Zb 143:8
m Zb 2:1
n Yos 2:24
Amo 9:5
o Yos 1:9
Yer 1:19
Ro 8:31
p Zb 9:9
q Zb 66:5
r Isa 34:2
s Isa 11:9
Mik 4:3
t Eze 39:9

Kwa kiongozi. Ya wana wa Kora[a]
juu ya Wanawali. Wimbo.
46 Kwetu Mungu ni kimbilio
na nguvu,[b]
Msaada unaopatikana kwa
utayari wakati wa
taabu.[c]
2 Ndiyo sababu hatutaogopa,
hata dunia ikibadilika[d]
Na hata milima ikitikisika
na kuingia katika moyo
wa bahari kuu;[e]
3 Hata maji yake yakiwa
na msukosuko, na kutoa
povu,[f]
Hata milima ikitikiswa na
ghasia yake.[g] *Sela*.
4 Kuna mto ambao vijito
vyake hulifanya jiji la
Mungu lishangilie,[h]
Maskani kuu takatifu zaidi
ya Aliye Juu Zaidi.[i]
5 Mungu yuko katikati ya
jiji;[j] halitatikisika.[k]
Mungu atalisaidia wakati
wa mapambazuko ya
asubuhi.[l]
6 Mataifa yakawa na
msukosuko,[m] falme
zikatikisika;
Akavumisha sauti yake,
dunia ikayeyuka.[n]
7 Yehova wa majeshi yuko
pamoja nasi;[o]
Mungu wa Yakobo ni kilele
chetu salama.[p] *Sela*
8 Njooni, tazameni matendo
ya Yehova,[q]
Jinsi ambavyo ameweka
matukio ya kushangaza
duniani.[r]
9 Anakomesha vita mpaka
kwenye mwisho wa
dunia.[s]
Upinde anauvunja
na kuukata mkuki
vipande-vipande;[t]

Magari ya kukokotwa anayateketeza motoni.[a]
10 "Salimuni amri, na mjue ya kwamba mimi ni Mungu.[b]
Nitatukuzwa kati ya mataifa,[c]
Nitatukuzwa duniani."[d]
11 Yehova wa majeshi yuko pamoja nasi;[e]
Mungu wa Yakobo ni kilele chetu salama.[f] *Sela*.

Kwa kiongozi. Ya wana wa Kora. Muziki.

47 Enyi vikundi vyote vya watu, pigeni makofi.[g]
Mpigieni Mungu kelele za ushindi kwa vigelegele vya shangwe.[h]
2 Kwa maana Yehova, Aliye Juu Zaidi, ni mwenye kuogopesha,[i]
Mfalme mkuu juu ya dunia yote.[j]
3 Atatiisha vikundi vya watu chini yetu[k]
Na vikundi vya mataifa chini ya miguu yetu.[l]
4 Atatuchagulia urithi wetu,[m]
Fahari ya Yakobo, ambaye amempenda.[n] *Sela*.
5 Mungu amepanda juu kwa vigelegele vya shangwe,[o]
Yehova kwa sauti ya baragumu.[p]
6 Mpigieni Mungu muziki, pigeni muziki.[q]
Mpigieni Mfalme wetu muziki, pigeni muziki.
7 Kwa maana Mungu ni Mfalme wa dunia yote;[r]
Pigeni muziki, mkitenda kwa busara.[s]
8 Mungu amekuwa mfalme juu ya mataifa.[t]
Mungu mwenyewe ameketi juu ya kiti chake kitakatifu cha ufalme.[u]

SURA 46

a Mik 5:10
b Hab 2:20
c Isa 2:11
d 1Nya 29:11
Zb 57:5
Yer 16:19
e 2Nya 20:17
f Zb 48:3
Zb 125:2

SURA 47

g 2Fa 11:12
Zb 98:4
Isa 55:12
h Ezr 3:11
Zb 33:3
i Kum 7:21
Ne 1:5
Zb 76:12
j Zb 22:28
Mal 1:14
k Zb 18:47
l Kum 33:29
m Kum 9:5
n Kum 7:6
Mal 1:2
o Zb 68:24
p 1Nya 15:24
q 1Nya 16:9
Zb 68:32
r Yer 10:7
Zek 14:9
s 1Ko 14:15
t 1Nya 16:31
Zb 96:10
Zb 97:1
Ufu 19:6
u Ufu 4:2

Safu ya 2

a Zb 110:3
b Ro 4:12
Ga 3:29
c Zb 89:18
d Zb 97:9

SURA 48

e Zb 42:Uta
f Ne 9:5
Zb 89:1
Zb 145:3
Zb 147:5
g Zb 46:4
Zb 87:3
h Zek 8:3
i Zb 50:2
Omb 2:15
j Isa 14:13
k Zb 47:8
Zb 135:21
Mt 5:35
l Zb 125:1
Zek 2:5
m 2Sa 10:6
2Sa 10:19
n Ufu 19:19
o Kut 14:25
p Kut 15:15
Isa 13:8
Da 5:6
q Yer 30:6
Ho 13:13
r 1Fa 22:48
Isa 2:16
Yer 18:17
Eze 27:26
s Zb 44:1
t Zb 48:1
Ebr 12:22

9 Wakuu wa watu wamekusanyika pamoja,[a]
Pamoja na watu wa Mungu wa Abrahamu.[b]
Kwa maana ngao za dunia ni za Mungu.[c]
Yeye amepanda juu sana.[d]

Wimbo. Muziki wa wana wa Kora.[e]

48 Yehova ni mkuu na wa kusifiwa sana[f]
Katika jiji la Mungu wetu,[g] katika mlima wake mtakatifu.[h]
2 Wenye ukuu wa kupendeza, shangwe ya dunia yote,[i]
Ni Mlima Sayuni ulioko sehemu za mbali za kaskazini,[j]
Mji wa Mfalme Mkuu.[k]
3 Katika minara ya makao yake Mungu amejulikana kuwa kilele salama.[l]
4 Kwa maana, Tazama! wafalme wenyewe wamekutana kwa mapatano,[m]
Wamepita karibu wakiwa pamoja.[n]
5 Wao wenyewe waliona; nao wakashangaa.
Wakasumbuka, wakakimbizwa wakiwa na wasiwasi mkubwa.[o]
6 Wakashikwa na kutetemeka wakiwa huko,[p]
Uchungu wa kuzaa kama ule wa mwanamke anayezaa.[q]
7 Kwa upepo wa mashariki wewe unavunja meli za Tarshishi.[r]
8 Kama vile tulivyosikia, ndivyo tumeona[s]
Katika jiji la Yehova wa majeshi, katika jiji la Mungu wetu.[t]

Mungu mwenyewe
atalifanya imara mpaka
wakati usio na kipimo.[a]
Sela
9 Tumefikiria kwa uzito, Ee
Mungu, juu ya fadhili
zako zenye upendo[b]
Katikati ya hekalu lako.[c]
10 Kama jina lako,[d] Ee Mungu,
ndivyo ilivyo sifa yako
Mpaka kwenye miisho ya
dunia.
Mkono wako wa kuume
umejaa uadilifu.[e]
11 Mlima Sayuni[f] na
ushangilie,
Miji ya kandokando ya
Yuda na ishangilie,[g] kwa
sababu ya maamuzi yako
ya hukumu.[h]
12 Pigeni mwendo
mkizunguka Sayuni, na
kuuzunguka-zunguka;[i]
Hesabuni minara yake.[j]
13 Wekeni mioyo yenu juu ya
boma lake.[k]
Kagueni minara ya makao
yake,
Ili mpate kukisimulia
kizazi cha wakati ujao.[l]
14 Kwa maana Mungu huyu
ni Mungu wetu mpaka
wakati usio na kipimo,
naam, milele.[m]
Yeye mwenyewe
atatuongoza mpaka
tufe.[n]

Kwa kiongozi.
Ya wana wa Kora.[o] Muziki.

49 Sikieni hili, enyi vikundi
vyote vya watu.
Tegeni sikio, enyi wakaaji
wote wa mfumo wa
mambo,[p]
2 Enyi wana wa wanadamu,
naam, ninyi wana wa
binadamu.
Wewe tajiri pamoja nawe
maskini.[q]

SURA 48

a Zb 87:5
Isa 2:2
Mik 4:1
b Zb 26:3
Zb 40:10
Zb 63:3
c 1Sa 3:3
2Sa 7:2
1Nya 16:1
Zb 63:2
d Kum 28:58
Zb 113:3
e Amu 5:11
Zb 17:7
Zb 60:5
Zb 98:2
f Zb 78:68
Yoe 2:32
g Zb 97:8
h 2Nya 20:27
Zb 137:8
Ufu 15:4
i Ne 12:31
j Ne 12:39
Isa 33:18
k Isa 26:1
l Kum 11:19
m Zb 31:14
n Isa 58:11

SURA 49

o 1Nya 6:37
p Zb 17:14
Ebr 1:2
q Zb 62:9

Safu ya 2

a Met 16:23
Mhu 10:12
b Zb 143:5
Met 14:33
Mt 12:35
Flp 4:8
c Zb 78:2
Mt 13:35
d Met 1:6
e Zb 27:1
Efe 5:16
f 2Sa 15:12
g Kum 8:17
Zb 52:7
Met 10:15
Met 18:11
1Ti 6:17
1Yo 2:16
h Est 5:11
Yer 9:23
Lu 12:19
i Met 11:4
Mt 16:26
j Ayu 36:18
k Zb 89:48
l Mhu 2:16
Ro 5:12
m Mhu 3:19
n Zb 39:6
Met 11:4
Met 23:4
Mhu 2:18
Yer 17:11
Lu 12:20
o Ayu 21:9
Zb 17:14
p Mhu 1:4
q Mwa 4:17
1Sa 15:12
2Sa 18:18

3 Kinywa changu mwenyewe
kitasema mambo ya
hekima,[a]
Na moyo wangu utatafakari
mambo ya uelewaji.[b]
4 Nitatega sikio langu nisikie
maneno ya kimethali;[c]
Nitafumbua kitendawili[d]
changu kwa kinubi.
5 Kwa nini niogope katika
siku za uovu,[e]
Wakati ambapo kosa la
wanaonipindua
linanizingira?[f]
6 Wale wanaotegemea riziki
zao,[g]
Na ambao wanaendelea
kujisifu juu ya wingi wa
utajiri wao,[h]
7 Hakuna hata mmoja wao
anayeweza kumkomboa
hata ndugu,[i]
Wala kumpa Mungu fidia
kwa ajili yake;
8 (Nayo bei ya ukombozi
wa nafsi yao ni yenye
thamani sana[j]
Hivi kwamba imekoma
mpaka wakati usio na
kipimo)
9 Hivi kwamba yeye aendelee
kuishi milele na asilione
shimo.[k]
10 Kwa maana yeye huona
kwamba hata wenye
hekima wanakufa,[l]
Mjinga na asiyetumia
akili huangamia wote
pamoja,[m]
Nao hulazimika kuwaachia
wengine mali yao.[n]
11 Tamaa yao ya ndani
ni kwamba nyumba zao
ziwepo mpaka wakati
usio na kipimo,[o]
Maskani zao mpaka kizazi
baada ya kizazi.[p]
Wameyaita mashamba yao
kwa majina yao.[q]

12 Na bado mtu wa udongo,
ingawa katika heshima,
hawezi kuendelea
kukaa;[a]
Kwa kweli analingana
na wanyama ambao
wameangamizwa.[b]
13 Hiyo ndiyo njia ya wale
wenye ujinga,[c]
Na ya wale wanaowafuata
ambao wanapendezwa na
maneno yao wenyewe.
Sela.
14 Kama kondoo, wao
wamewekewa Kaburi;*[d]
Kifo chenyewe
kitawachunga;[e]
Nao wanyoofu
watawatawala asubuhi,[f]
Nayo maumbo yao
hayatakosa kuchakaa;[g]
Kaburi* badala ya makao
yaliyo juu ni kwa ajili ya
kila mmoja.[h]
15 Hata hivyo, Mungu
mwenyewe ataikomboa
nafsi yangu kutoka
katika mkono wa
Kaburi,*[i]
Kwa maana atanipokea.
Sela.
16 Usiogope kwa sababu mtu
fulani anapata utajiri,[j]
Kwa sababu utukufu
wa nyumba yake
unaongezeka,[k]
17 Kwa maana anapokufa
hawezi kuchukua kitu
chochote;[l]
Utukufu wake hautashuka
chini pamoja naye.[m]
18 Kwa maana muda wote
wa maisha yake alikuwa
akiibariki nafsi yake
mwenyewe;[n]
(Na watu watakusifu kwa
sababu unajiendeleza
vizuri)[a]
19 Nafsi yake mwishowe
inafikia tu kwenye kizazi
cha mababu zake.[b]
Hawataona nuru tena
kamwe.[c]
20 Mtu wa udongo, ingawa
katika heshima, ambaye
haelewi,[d]
Kwa kweli analingana
na wanyama ambao
wameangamizwa.[e]

Muziki wa Asafu.[f]

50 Mwenye Uwezo,[g] Mungu,
Yehova,[h] amesema
mwenyewe,[i]
Naye anaiita dunia,[j]
Kutoka mashariki mpaka
magharibi.[k]
2 Kutoka Sayuni, ukamilifu
wa uzuri,[l] Mungu
mwenyewe ameangaza.[m]
3 Mungu wetu atakuja naye
hawezi kukaa kimya.[n]
Mbele zake kuna moto
unaoteketeza,[o]
Na kumzunguka pande
zote hali ya hewa
imekuwa yenye dhoruba
kali sana.[p]
4 Yeye anaziita mbingu juu
na dunia[q]
Ili atekeleze hukumu juu ya
watu wake:[r]
5 "Wakusanye kwangu
washikamanifu wangu,[s]
Wale wanaofanya agano
langu juu ya dhabihu."[t]
6 Na mbingu zinasema juu ya
uadilifu wake,[u]
Kwa maana Mungu
mwenyewe ni Mwamuzi.[v]
Sela.
7 "Sikilizeni, enyi watu
wangu, nami nitasema,[w]

SURA 49
a Zb 39:5 Yak 1:11
b Mhu 3:20
c Lu 12:20
d Ayu 21:13
e Ayu 24:19 Ro 5:14 Ufu 6:8
f Zb 30:5 Mal 4:3
g Zb 39:11
h 1Sa 2:6 Ayu 7:9
i Ayu 33:28 Zb 16:10 Zb 30:3 Zb 56:13 Zb 86:13
j Est 3:1
k Est 5:11
l Ayu 1:21 Mhu 5:15 Lu 12:20 1Ti 6:17
m Isa 10:3
n Kum 29:19 Lu 12:19

Safu ya 2
a Met 14:20
b Mwa 15:15
c Ayu 33:30 Zb 56:13
d Ayu 4:21 Zb 49:12 Met 16:16
e Mhu 3:19 2Pe 2:12

SURA 50
f 1Nya 15:17
g Yos 22:22 Isa 46:9 Yer 32:18
h Zb 95:3
i Amo 3:8
j Isa 1:2
k Isa 45:6
l Zb 48:2 Omb 2:15
m Kum 33:2 Zb 80:1
n Zb 83:1 Isa 42:13 Isa 65:6
o Kut 19:18 Zb 97:3 Da 7:10 Ebr 12:29
p Zb 97:4
q Kum 4:36 Kum 30:19 Kum 32:1 Isa 1:2
r Mik 6:2 Ebr 10:30
s Kum 33:3 2Nya 29:20 Zb 14:7 Met 2:8 Isa 13:3
t Kut 24:8 Lu 22:20 Yoh 11:52
u Zb 97:6
v Zb 7:11 Zb 75:7 Ebr 12:23 Ufu 20:12
w Zb 81:8

Zb 49:14,* 15* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

Ee Israeli, nami nitatoa
ushahidi dhidi yako.[a]
Mimi ni Mungu, Mungu
wako.[b]
8 Mimi siwakaripii
kuhusiana na dhabihu
zenu,[c]
Wala kuhusiana na
matoleo yako mazima ya
kuteketezwa yaliyo
mbele zangu daima.[d]
9 Sitachukua ng'ombe-dume
katika nyumba yako,[e]
Wala mbuzi-dume katika
mazizi yako.
10 Kwa maana kila mnyama
wa mwituni ni wangu,[f]
Wanyama walio juu ya
milima elfu moja.[g]
11 Najua vizuri kila kiumbe
chenye mabawa cha
milimani,[h]
Na makundi ya wanyama
wa porini yako pamoja
nami.[i]
12 Ningalikuwa na njaa,
singalikuambia;
Kwa maana nchi yenye
kuzaa[j] na vyote
vinavyoijaza ni vyangu.[k]
13 Je, nile nyama ya
ng'ombe-dume wenye
nguvu,[l]
Na je, ninywe damu ya
mbuzi-dume?[m]
14 Toa shukrani zikiwa
dhabihu yako kwa
Mungu,[n]
Na umtimizie Aliye Juu
Zaidi nadhiri zako;[o]
15 Na uniite katika siku ya
taabu.[p]
Nitakuokoa, nawe
utanitukuza."[q]
16 Lakini Mungu
atamwambia mwovu:[r]
"Una haki gani ya kuyataja
masharti yangu,[s]
Na kwamba ulichukue
agano langu kinywani
mwako?[a]
17 Tazama, wewe—wewe
umechukia nidhamu,[b]
Nawe unaendelea
kuyatupa maneno
yangu nyuma yako.[c]
18 Wakati wowote
ulipomwona mwizi,
naam, ulipendezwa
naye;[d]
Nawe ulishirikiana na
wazinzi.[e]
19 Umefungua kinywa chako
kutoa lililo baya,[f]
Na ulimi wako
unaushikamanisha na
udanganyifu.[g]
20 Unaketi na kusema vibaya
juu ya ndugu yako
mwenyewe,[h]
Juu ya mwana wa mama
yako unafichua kosa.[i]
21 Umeyafanya mambo hayo,
nami nikaendelea kukaa
kimya.[j]
Ulidhani kwamba kwa
hakika mimi ningekuwa
kama wewe.[k]
Nitakukaripia,[l] nami
nitayarekebisha mambo
mbele ya macho yako.[m]
22 Tafadhali, enyi
mnaomsahau Mungu
eleweni hili,[n]
Nisije nikawararua
vipande-vipande bila ya
kuwa na mkombozi.[o]
23 Yule anayetoa shukrani
zikiwa dhabihu yake
ndiye anayenitukuza;[p]
Naye anayedumisha njia
iliyowekwa,
Nitamfanya aone wokovu
wa Mungu."[q]

SURA 50

a Ne 9:30
b Kut 20:2
c Zb 40:6
Isa 1:11
Yer 7:22
d 1Sa 15:22
Ho 6:6
e Mik 6:7
f Mwa 1:24
1Nya 29:14
Ayu 40:15
g Mdo 17:24
h Mwa 1:20
Ayu 38:41
Zb 104:12
Mt 10:29
i Zb 80:13
j 1Sa 2:8
Zb 24:1
Zb 89:11
k Kut 19:5
Kum 10:14
Ayu 41:11
Zb 104:24
1Ko 10:26
l Ho 14:2
m Mik 6:6
n Zb 69:30
Zb 107:22
Met 21:3
Ho 6:6
Ebr 13:15
o Kum 23:21
Zb 15:4
Zb 76:11
Mhu 5:4
Yon 2:9
Mt 5:33
p 2Nya 33:12
Zb 77:2
Zb 91:15
Lu 22:44
q Zb 22:23
Zb 50:23
r Isa 48:1
Eze 18:27
s Yer 7:4
Mt 7:23
Ro 2:21

Safu ya 2

a Kum 29:21
Kum 31:20
Ebr 8:9
b Met 1:7
Met 5:12
Ebr 12:6
c Ne 9:26
Isa 5:24
Yer 8:9
d Isa 5:23
Ro 1:32
Ro 2:21
e Yak 4:4
2Yo 11
f Zb 52:3
Yer 9:5
g Zb 52:2
Yak 3:5
h Law 19:16
Zb 31:18
Lu 22:65
i Mt 10:21
j Mhu 8:11
Ro 2:4
2Pe 3:9
k Hes 23:19
Zb 73:11
Zb 94:7
Mhu 8:12
l Met 29:1
m Zb 50:4
Mhu 12:14
n Zb 9:17
Isa 51:13
Yer 2:32
Ho 4:6

o Zb 7:2; p Zb 22:23; Zb 27:6; Ro 12:1; Efe 5:20; 1Th 5:18; Ebr 13:15; q Zb 91:16; Mik 6:8; Lu 2:30.

Kwa kiongozi. Muziki wa Daudi. Nathani nabii alipoingia kwake baada ya Daudi kulala na Bath-sheba.[a]

51 Ee Mungu, unionyeshe kibali kulingana na fadhili zako zenye upendo.[b]
Ufutilie mbali makosa yangu kulingana na wingi wa rehema zako.[c]
2 Unioshe kabisa kutokana na kosa langu,[d]
Na kunitakasa kutokana na dhambi yangu.[e]
3 Kwa maana mimi mwenyewe nayajua makosa yangu,[f]
Na dhambi yangu iko mbele yangu daima.[g]
4 Dhidi yako wewe, wewe peke yako, nimetenda dhambi,[h]
Nami nimefanya lililo baya machoni pako,[i]
Ili uwe mwadilifu unapoongea,[j]
Ili usiwe na lawama unapohukumu.[k]
5 Tazama! Nilizaliwa kwa maumivu nikiwa na kosa,[l]
Na mama yangu alinichukua mimba katika dhambi.[m]
6 Tazama! Umependezwa na ukweli wenyewe katika sehemu za ndani;[n]
Na katika mtu wa sirini unijulishe hekima tupu.[o]
7 Unitakase kwa hisopo kutokana na dhambi, ili nipate kuwa safi;[p]
Unioshe, ili nipate kuwa mweupe kuliko theluji.[q]
8 Unifanye nisikie kufurahi na kushangilia,[r]
Ili mifupa uliyoiponda ipate kuwa na shangwe.[s]

SURA 51

a 2Sa 11:3
b Hes 14:18 Zb 25:7 Zb 32:10 Zb 41:4 Zb 90:14 Zb 103:11
c Zb 39:8 Zb 103:13 Met 28:13 Isa 43:25 Isa 44:22
d Isa 1:18 1Ko 6:11
e Ebr 9:14 1Yo 1:7
f Zb 32:5
g Zb 40:12
h Mwa 20:6 Mwa 39:9 Law 5:19 2Sa 12:13 Lu 15:21
i 2Sa 12:9 Zb 38:18
j Zb 50:6 Ro 3:4
k Lu 7:29 Ufu 19:2
l Mwa 3:16 Ayu 14:4 Ro 5:12
m Ro 3:23 Efe 2:3
n 2Fa 20:3 1Nya 29:17
o 1Sa 16:7 1Pe 3:4
p Law 14:4 Hes 19:18 Ebr 9:14
q Isa 1:18
r Zb 30:11
s Zb 6:2 Zb 38:3 Isa 57:15

Safu ya 2

a Zb 103:12 Isa 38:17 Yer 16:17
b Mik 7:19
c Yer 32:39 Mdo 15:9 Efe 2:10
d Eze 11:19 Efe 4:23
e Mwa 4:14 2Fa 13:23 Zb 102:10
f Lu 11:13 Ro 8:9 Efe 4:30
g Zb 21:1 Lu 1:47
h Zb 110:3 Mt 26:41
i Mdo 2:38
j Mdo 3:19
k Mwa 9:6 1Sa 25:34 Zb 26:9 Eze 33:8 Mdo 18:6 Mdo 20:26
l Zb 38:22 Zb 88:1 Isa 12:2 Ufu 7:10
m Ne 9:33 Zb 20:5 Zb 35:28 Zb 59:16 Da 9:7 Ro 10:3
n Eze 3:27

9 Ufiche uso wako kutoka kwa dhambi zangu,[a]
Na ufutilie mbali makosa yangu yote.[b]
10 Uumbe moyo safi ndani yangu, Ee Mungu,[c]
Na kuweka ndani yangu roho mpya, iliyo imara.[d]
11 Usinitupilie mbali na uso wako;[e]
Wala usiniondolee roho yako takatifu.[f]
12 Unirudishie shangwe ya wokovu wako,[g]
Nawe unitegemeze kwa roho ya kupenda.[h]
13 Nitawafundisha wakosaji njia zako,[i]
Ili watenda-dhambi wageuke na kurudi kwako kabisa.[j]
14 Unikomboe kutokana na hatia ya damu,[k] Ee Mungu, Mungu wa wokovu wangu,[l]
Ili ulimi wangu upate kutangaza uadilifu wako kwa shangwe.[m]
15 Ee Yehova, na uifungue hii midomo yangu,[n]
Ili kinywa changu mwenyewe kipate kutangaza sifa yako.[o]
16 Kwa maana hupendezwi na dhabihu—kama sivyo ningeitoa;[p]
Hupendezwi na toleo zima la kuteketezwa.[q]
17 Dhabihu kwa Mungu ni roho iliyovunjika;[r]
Moyo uliovunjika na kupondwa, Ee Mungu, hutaudharau.[s]
18 Kwa nia yako njema utendee Sayuni vema;[t]

o Zb 34:1; Zb 71:8; Zb 109:30; Zb 145:21; Ebr 13:15; p 1Sa 15:22; Met 21:3; Ho 6:6; q Zb 40:6; Zb 50:8; Isa 1:11; Yer 7:22; Amo 5:22; r 2Fa 22:19; Zb 34:18; Isa 57:15; Lu 18:13; s 2Nya 33:13; Zb 22:24; Zb 119:58; Met 28:13; Lu 15:22; t Zb 102:16; Isa 62:1.

Na ujenge kuta za
Yerusalemu.[a]
19 Ndipo utakapopendezwa na
dhabihu za uadilifu,[b]
Na dhabihu za
kuteketezwa na toleo
zima;[c]
Ndipo ng’ombe-dume
watakapotolewa katika
madhabahu yako
mwenyewe.[d]

Kwa kiongozi. Maskili. Ya Daudi, wakati Doegi Mwedomu alipokuja na kumwambia Sauli kwamba Daudi alikuwa ameenda kwenye nyumba ya Ahimeleki.[e]

52 Kwa nini unajisifia yaliyo
mabaya, ewe mwenye
nguvu?[f]
Fadhili zenye upendo za
Mungu ni za mchana
kutwa.[g]
2 Ulimi wako hupanga hila
za kuleta shida, ukiwa
umenolewa kama
wembe,[h]
Ukifanya kazi kwa
udanganyifu.[i]
3 Umependa yaliyo mabaya
kuliko yaliyo mema,[j]
Kusema uwongo kuliko
kusema yaliyo ya
uadilifu.[k] *Sela*.
4 Umependa maneno yote
yenye kumeza,[l]
Ewe ulimi wenye
udanganyifu.[m]
5 Mungu mwenyewe pia
atakubomoa milele;[n]
Atakupiga na
kukuangusha na
kukurarua kutoka
katika hema lako,[o]
Naye atakung’oa kutoka
katika nchi ya walio hai.[p]
Sela.
6 Nao waadilifu wataona hilo
na kuogopa,[q]
Nao watamcheka.[r]

SURA 51

a Da 9:25
Mik 7:11
b Mal 3:3
c Zb 4:5
Ro 12:1
d Ho 14:2

SURA 52

e 1Sa 22:9
f Mwa 10:8
1Sa 21:7
Zb 94:4
g Zb 103:17
h Zb 50:19
Zb 57:4
Zb 59:7
Zb 64:3
i Zb 109:2
2Ko 11:13
j Yer 4:22
Mik 3:2
k Zb 62:4
Yer 9:3
Yoh 8:44
l 1Sa 22:18
m Met 14:25
Yak 3:6
1Pe 3:10
n Zb 55:23
Met 12:19
Met 15:25
Met 19:9
o Zb 28:5
Zb 37:9
p Met 2:22
q Zb 37:34
Zb 40:3
Zb 119:120
Mal 1:5
Ufu 19:2
r Zb 58:10
Isa 37:22
Ufu 18:20

Safu ya 2

a Zb 146:3
Yer 17:5
b Zb 49:6
Met 11:28
Met 23:5
1Ti 6:17
c Mhu 8:8
d Yer 11:16
Ho 14:6
e Zb 13:5
Zb 147:11
f Zb 50:15
g Zb 27:14
Zb 54:6
Zb 123:2
Met 18:10

SURA 53

h Zb 88:Uta
i Zb 10:4
Zb 14:1
Zb 92:6
Ro 1:21
j Mwa 6:11
Law 18:30
Kum 32:5
k Zb 14:3
Ro 3:10
l Zb 8:4
Zb 11:4
Zb 33:14
Zb 102:19
Yer 16:17
Yer 23:24

7 Huyo ndiye mwanamume
ambaye hamweki Mungu
kuwa ngome yake,[a]
Lakini anategemea wingi
wa utajiri wake,[b]
Ambaye hulindwa
kutokana na shida
anazoleta.[c]
8 Lakini nitakuwa kama
mzeituni[d] wenye majani
mengi katika nyumba ya
Mungu;
Nazitegemea fadhili zenye
upendo za Mungu mpaka
wakati usio na kipimo,
naam, milele.[e]
9 Nitakusifu mpaka wakati
usio na kipimo, kwa
maana wewe umechukua
hatua;[f]
Nami nitalitumainia jina
lako, kwa sababu ni jema,
mbele ya washikamanifu
wako.[g]

Kwa kiongozi juu ya Mahalathi.[h] Maskili. Ya Daudi.

53 Asiye na akili amesema
katika moyo wake:
“Hakuna Yehova.”[i]
Wametenda kwa uharibifu
na kutenda kwa njia
yenye kuchukiza katika
ukosefu wa uadilifu;[j]
Hakuna yeyote anayefanya
mema.[k]
2 Kutoka mbinguni Mungu
amewatazama wana wa
binadamu walio chini,[l]
Aone kama kuna yeyote
ambaye ana ufahamu,
yeyote anayemtafuta
Yehova.[m]
3 Wote wamegeuka nyuma,
wote ni wafisadi katika
njia ileile;[n]

m 1Nya 28:9; 2Nya 15:2; 2Nya 19:3; Ayu 28:28; Isa 55:6; 1Pe 3:12; n Mwa 6:5; Isa 53:6; Yer 8:6; Sef 1:6.

Hakuna yeyote anayefanya mema,[a]
Hakuna hata mmoja.
4 Je, hakuna yeyote kati ya wale wanaotenda mambo yenye kuumiza ambaye ana ujuzi,[b]
Wakila watu wangu kama vile ambavyo wamekula mkate?[c]
Hata hawajamwitia Yehova.[d]
5 Hapo wamejawa na hofu kubwa,[e]
Mahali ambapo hapakuwa na kitu chenye kutia hofu;[f]
Kwa maana hakika Mungu ataitawanya mifupa ya mtu yeyote anayepiga kambi dhidi yako.[g]
Hakika utawafanya waone aibu, kwa maana Yehova mwenyewe amewakataa.[h]
6 Laiti wokovu mkuu wa Israeli ungetoka Sayuni![i]
Wakati ambapo Yehova anawakusanya tena mateka wa watu wake,[j]
Yakobo na ashangilie, Israeli na afurahi.[k]

5 Ili nipate kuona wema kwa
wachaguliwa wako,[l]
Ili nipate kushangilia
kwa shangwe ya taifa
lako,[m]
Ili nipate kujisifu pamoja
na urithi wako.[n]
6 Tumetenda dhambi kama
mababu zetu;[o]
Tumefanya kosa;
tumetenda kwa uovu.[p]
7 Mababu zetu huko Misri,
Hawakuonyesha ufahamu
wowote katika kazi zako
za ajabu.[q]
Hawakukumbuka wingi
wa fadhili zako kuu
zenye upendo,[r]
Bali walijiendesha kwa
uasi penye bahari, kando
ya Bahari Nyekundu.[s]

SURA 105

a Kut 12:29 Zb 78:51 Zb 135:8
b Mwa 49:3
c Mwa 15:14 Kut 3:22 Kut 12:35
d Kut 11:7 Kut 12:33
e Kut 14:20
f Kut 13:21 Hes 9:15 Ne 9:12 Zb 78:14
g Kut 16:13 Hes 11:32 Zb 78:27
h Kut 16:15 Zb 78:24
i Kut 17:6 1Ko 10:4
j Zb 78:16 Isa 48:21
k Mwa 12:7 Mwa 15:14 Kut 2:24 Kum 9:5 Lu 1:72
l Hes 33:3 Mdo 13:17
m Zb 106:12 Isa 51:10
n Kum 6:10 Yos 11:23 Yos 21:43 Ne 9:22 Zb 78:55 Zb 135:12 Mdo 7:45 Mdo 13:19
o Kum 6:10 Yos 5:11 Zb 44:2
p Kum 4:40 Kum 6:1

Safu ya 2

a Zb 19:7
b Zb 150:1 Ufu 19:6

SURA 106

c Zb 117:1
d 1Nya 16:34 Ezr 3:11 Zb 107:1 Lu 18:19 1Th 5:18
e Zb 103:17
f Zb 40:5
g Ne 9:5
h Zb 119:2 Isa 56:1
i Zb 15:2 Isa 64:5 Mdo 24:16 Ga 6:9
j Ne 5:19 Zb 51:18 Zb 119:132 Lu 2:14
k Zb 3:8
l Kut 19:5 1Pe 2:9
m Zb 14:7
n Yer 9:24 1Ko 1:31
o Law 26:40 Ne 9:16 Zb 78:8
p 1Fa 8:47 Ezr 9:6 Da 9:5
q Isa 44:18
r Zb 78:42; Isa 63:7; s Kut 14:11.

8 Naye akawaokoa kwa ajili
ya jina lake,[a]
Ili kufanya nguvu zake
zijulikane.[b]
9 Kwa hiyo akaikemea
Bahari Nyekundu, nayo
ikakauka hatua kwa
hatua;[c]
Naye akawatembeza
kupita katika kilindi cha
maji kana kwamba ni
nyikani;[d]
10 Na kwa hiyo akawaokoa
kutoka katika mkono wa
mchukiaji[e]
Na kuwakomboa kutoka
katika mkono wa adui.[f]
11 Na maji yakaja
kuwafunika wapinzani
wao;[g]
Hakuna hata mmoja wao
aliyebaki.[h]
12 Kisha wakawa na imani
katika neno lake;[i]
Wakaanza kuimba sifa
yake.[j]
13 Upesi wakasahau kazi
zake;[k]
Hawakungojea shauri
lake.[l]
14 Lakini walionyesha tamaa
yao ya ubinafsi nyikani[m]
Na kumjaribu Mungu
jangwani.[n]
15 Naye akawapa ombi lao[o]
Na kuwatumia ugonjwa
unaodhoofisha ndani ya
nafsi yao.[p]
16 Nao wakaanza kumwonea
Musa wivu katika
kambi,[q]
Hata Haruni mtakatifu wa
Yehova.[r]
17 Kisha dunia ikafunguka na
kummeza Dathani,[s]
Na kulifunika kusanyiko
la Abiramu.[t]

SURA 106

a Yos 7:9
Zb 143:11
Eze 20:14
b Kut 9:16
Ro 9:17
c Kut 14:21
Yos 2:10
Ne 9:11
Zb 66:6
Zb 78:13
Zb 136:13
d Ne 9:11
Zb 77:19
Zb 136:14
Isa 63:13
e Kut 14:30
Lu 1:71
f Isa 41:11
Isa 49:26
Mik 6:4
g Kut 14:28
Kut 15:5
Kum 11:4
Yos 24:7
Zb 78:53
h Kut 14:13
i Kut 14:31
j Kut 15:1
k Kut 15:24
Kut 16:2
Kut 17:7
Zb 78:11
l Isa 48:18
m Hes 11:4
Kum 9:22
1Ko 10:6
n Kut 17:2
Hes 14:22
Zb 78:18
1Ko 10:9
Ebr 3:9
o Hes 11:31
Zb 78:29
p Hes 11:33
q Hes 16:3
r Law 21:8
Hes 16:7
s Hes 16:32
t Hes 16:27
Hes 26:10
Kum 11:6

Safu ya 2

a Hes 16:35
b Ebr 12:29
c Kut 32:4
Ne 9:18
d Kum 9:12
e Isa 42:8
Yer 2:11
f Kut 20:4
Ro 1:23
g Kum 32:18
Zb 78:42
h Kum 4:34
Zb 135:9
i Zb 78:51
Zb 105:27
j Kut 14:25
k Kut 32:10
Kum 9:14
Eze 20:13
l Kut 32:11
Kum 9:19
Yak 5:16
m Eze 22:30
n Hes 13:32
Kum 8:7
Yer 3:19
Eze 20:6
o Hes 14:11
Ebr 3:19
p Hes 14:2
Hes 14:27
Kum 1:27
q Hes 14:22

18 Na moto ukawaka katikati
ya kusanyiko lao;[a]
Mwali wa moto
ukawateketeza waovu.[b]
19 Na zaidi ya hayo,
wakatengeneza ndama
katika Horebu[c]
Na kuinamia sanamu ya
kuyeyushwa,[d]
20 Hivi kwamba wakabadili
utukufu wangu[e]
Kwa ajili ya mfano wa
ng'ombe mwenye kula
majani.[f]
21 Walimsahau Mungu
Mwokozi wao,[g]
Mtendaji wa mambo
makuu nchini Misri,[h]
22 Kazi za ajabu katika nchi
ya Hamu,[i]
Mambo yenye kuogopesha
kwenye Bahari
Nyekundu.[j]
23 Naye alikuwa karibu
kusema waangamizwe,[k]
Isingalikuwa ni kwa
sababu ya Musa
mchaguliwa wake,
Aliyesimama penye
mwanya mbele zake,[l]
Ili kuigeuza ghadhabu
yake asiwaharibu.[m]
24 Nao wakaichukia nchi
yenye kutamanika;[n]
Hawakuwa na imani
katika neno lake.[o]
25 Nao wakaendelea
kunung'unika katika
mahema yao;[p]
Hawakuisikiliza sauti ya
Yehova.[q]
26 Kwa hiyo akainua mkono
wake katika kiapo juu
yao,[r]
Kwamba angewafanya
waanguke nyikani,[s]

r Kut 6:8; Ebr 3:11; s Hes 14:29.

27 Na kwamba angefanya
uzao wao uanguke kati
ya mataifa,[a]
Na kwamba
angewatawanya katika
nchi mbalimbali.[b]
28 Nao wakaanza
kujishikamanisha na
Baali wa Peori[c]
Na kula dhabihu za wafu.[d]
29 Walipokuwa
wakisababisha uchungu
kwa matendo yao,[e]
Tauni ikazuka katikati
yao.[f]
30 Finehasi aliposimama na
kuingilia kati,[g]
Ndipo tauni ikazuiwa.
31 Na ikahesabiwa kwake
kuwa ni uadilifu
Kwa kizazi baada ya kizazi
mpaka wakati usio na
kipimo.[h]
32 Tena, wakafanya uchokozi
katika maji ya Meriba,[i]
Hivi kwamba mambo
yakamwendea Musa
vibaya kwa sababu yao.[j]
33 Kwa maana waliitia
uchungu roho yake
Naye akaanza kusema
kwa midomo yake bila
kufikiri.[k]
34 Hawakuangamiza vikundi
vya watu,[l]
Kama Yehova alivyokuwa
amewaambia.[m]
35 Nao wakachangamana na
hayo mataifa[n]
Na kuanza kujifunza
matendo yao.[o]
36 Nao waliendelea
kutumikia sanamu zao,[p]
Nazo zikawa mtego kwao.[q]
37 Nao wakawa wakiwatoa
dhabihu wana wao[r]
Na binti zao kwa roho
waovu.[a]
38 Kwa hiyo wakaendelea
kumwaga damu isiyo na
hatia,[b]
Damu ya wana wao na
binti zao,
Ambao waliwatoa dhabihu
kwa sanamu za
Kanaani;[c]
Na nchi ikachafuliwa na
umwagaji wa damu.[d]
39 Nao wakawa wasio safi kwa
sababu ya kazi zao[e]
Na wakaendelea kufanya
uasherati kwa matendo
yao.[f]
40 Na hasira ya Yehova
ikaanza kuwaka juu ya
watu wake;[g]
Naye akaja kuuchukia
urithi wake.[h]
41 Naye akawatia mkononi
mwa mataifa tena na
tena,[i]
Ili wale wanaowachukia
wapate kutawala juu
yao,[j]
42 Na ili adui zao wapate
kuwakandamiza,
Na ili wapate kutiishwa
chini ya mkono wao.[k]
43 Akawakomboa mara
nyingi,[l]
Lakini wao wakawa
wakijiendesha kwa uasi
katika mwendo wao wa
kutokutii,[m]
Nao wakashushwa kwa
sababu ya kosa lao.[n]
44 Naye akaiona taabu yao[o]
Alipokisikia kilio chao
cha kusihi.[p]

SURA 106

a Kum 4:27
b Law 26:33
Zb 44:11
Eze 20:23
c Hes 25:3
Hes 31:16
Kum 4:3
Kum 32:17
Ho 9:10
d Zb 115:7
Ufu 2:14
e Hes 25:6
Kum 32:16
f Hes 25:9
1Ko 10:8
g Hes 25:8
Yos 7:12
h Hes 25:13
i Hes 20:2
Hes 27:14
Kum 32:51
j Hes 20:12
Kum 1:37
k Hes 20:10
Ayu 2:10
Zb 141:3
Met 16:32
Yak 3:2
l Yos 16:10
Yos 17:12
Amu 1:21
m Hes 33:52
Kum 7:2
Amu 2:2
n Yos 15:63
Amu 1:33
Ho 7:8
o Isa 2:6
1Ko 5:6
1Ko 15:33
p Amu 2:12
2Fa 17:12
Ho 4:17
q Kut 23:33
Amu 2:3
r Kum 12:31
2Fa 16:3
2Fa 17:17
Isa 57:5
Yer 7:31
Eze 16:20

Safu ya 2

a Kum 32:17
1Ko 10:20
b Kum 21:9
2Fa 21:16
Yer 2:34
Ho 12:14
c Eze 16:20
d Hes 35:33
Isa 26:21
e Isa 24:5
Eze 20:18
f Kut 34:16
Law 17:7
Hes 15:39
Yer 3:9
Eze 20:30
g Amu 2:14
Zb 78:59
h Kum 9:29
Kum 32:19
i Kum 32:30
Amu 3:8
j Amu 10:8
k Kum 28:25

l Amu 2:16; Amu 10:12; 1Sa 12:11; Ne 9:27; m Amu 4:1; Amu 5:8; Eze 2:3; n Amu 6:5; o Amu 2:18; p Amu 3:9; Amu 4:3; Amu 10:15; 1Sa 7:8; Ne 9:28.

45 Naye akalikumbuka
agano lake juu yao,[a]
Naye akajuta kulingana
na wingi wa fadhili
zake kuu zenye
upendo.[b]
46 Naye akawa akiwafanya
wahurumiwe
Mbele ya wale wote
waliokuwa
wamewashika
mateka.[c]
47 Utuokoe, Ee Yehova
Mungu wetu,[d]
Na utukusanye pamoja
kutoka kwa mataifa[a]
Ili tulishukuru jina lako
takatifu,[b]
Ili tukusifu kwa shangwe.[c]
48 Na abarikiwe Yehova
Mungu wa Israeli[d]
kutoka wakati usio na
kipimo mpaka wakati
usio na kipimo;[e]
Na watu wote waseme
Amina.[f]
Msifuni Yah!

SURA 106

a Law 26:42
2Fa 13:23
Zb 105:8
Lu 1:72
b Kut 34:6
Hes 14:18
Kum 32:36
Amu 2:18
2Sa 24:16
Zb 51:1
Zb 69:16
Zb 86:15
Zb 90:13
Isa 63:7
Omb 3:32
Yoe 2:13
c 1Fa 8:50
Ezr 9:9
Yer 42:12
d 1Nya 16:35
Zb 79:9

Safu ya 2

a Yer 32:37
Eze 36:24

b Zb 103:1; Zb 105:3; **c** Isa 43:21; **d** 1Nya 29:10; Zb 41:13; Lu 1:68; **e** 1Ko 14:16; **f** Zb 106:1.

KITABU CHA TANO
(Zaburi 107 – 150)

107 Mshukuruni Yehova,
kwa maana yeye ni
mwema;[a]
Kwa maana fadhili zake
zenye upendo ni za
mpaka wakati usio na
kipimo.[b]
2 Wote waliookolewa wa
Yehova na waseme
hivyo,[c]
Ambao amewaokoa kutoka
katika mkono wa adui,[d]
3 Na ambao amewakusanya
pamoja kutoka katika
nchi mbalimbali,[e]
Kutoka mashariki na
kutoka magharibi,[f]
Kutoka kaskazini na
kutoka kusini.[g]
4 Walitanga-tanga nyikani,[h]
jangwani;[i]
Hawakupata njia yoyote ya
kwenda kwenye jiji la
kukaa.[j]
5 Walikuwa na njaa, na kiu
pia;[k]
Nafsi yao ndani yao
ikaanza kuzimia.[l]
6 Nao wakaendelea kumlilia
Yehova katika taabu
yao;[a]
Akawakomboa kutoka
katika mikazo iliyokuwa
juu yao,[b]
7 Na kuwatembeza katika
njia iliyo sawa,[c]
Ili waingie katika jiji la
kukaa.[d]
8 Watu na wamtolee Yehova
shukrani kwa ajili ya
fadhili zake zenye
upendo[e]
Na kwa ajili ya kazi zake
za ajabu kwa wana wa
binadamu.[f]
9 Kwa maana ameishibisha
nafsi iliyokauka;[g]
Na nafsi yenye njaa
ameijaza vitu vyema.[h]
10 Kuna wale waliokuwa
wakikaa katika giza na
kivuli kizito,[i]
Wafungwa katika mateso
na vyuma.[j]

SURA 107

a 1Nya 16:34
Zb 118:1
Lu 18:19
b Zb 103:17
c Kum 15:15
Zb 31:5
Lu 1:68
1Pe 1:19
d Kum 7:8
Zb 106:10
Isa 35:10
Yer 15:21
Mik 4:10
Lu 1:74
e Zb 106:47
f Isa 43:5
Isa 49:12
Yer 29:14
Mt 24:31
g Isa 43:6
Yer 31:8
Eze 39:27
Lu 13:29
h Hes 14:33
Kum 8:15
i Kum 32:10
Ebr 11:38
j Ebr 11:10
k Kut 15:24
l Kut 16:3
Omb 2:19

Safu ya 2

a Zb 50:15
Zb 91:15
Ho 5:15
b Isa 41:17
2Ti 3:11
c Ezr 8:21
Zb 78:52
Isa 30:21
2Pe 2:21
d Ne 11:3
e 1Nya 16:8
Zb 136:1
f Zb 40:5
Ufu 15:3
g Isa 55:2
h Zb 34:10
Zb 146:7
Yer 31:14
Lu 1:53

i Lu 1:79; **j** 2Nya 33:11; Ayu 36:8; Zb 105:18; Zb 149:8.

11 Kwa maana waliyaasi[a]
maneno ya Mungu;[b]
Na shauri la Aliye
Juu Zaidi hawakuwa
wameliheshimu.[c]
12 Kwa hiyo, akautiisha moyo
wao kwa taabu;[d]
Walijikwaa, wala
hapakuwa na mtu
mwenye kusaidia.[e]
13 Nao wakaanza kumwomba
Yehova msaada katika
taabu yao;[f]
Na kutoka katika mikazo
iliyokuwa juu yao yeye
akawaokoa kama
kawaida.[g]
14 Akawatoa katika giza na
kivuli kizito,[h]
Na hata kuzikata pingu zao.[i]
15 Watu na wamshukuru
Yehova kwa ajili ya
fadhili zake zenye
upendo[j]
Na kwa ajili ya kazi zake
za ajabu kwa wana wa
binadamu.[k]
16 Kwa maana ameivunja
milango ya shaba,[l]
Naye ameyakata hata
mapingo ya chuma.[m]
17 Wale waliokuwa
wapumbavu, kwa sababu
ya njia ya ukosaji wao[n]
Na kwa sababu ya
makosa yao, mwishowe
walijiletea mateso
wenyewe.[o]
18 Nafsi yao ikachukia kila
namna ya chakula,[p]
Nao wakayafikia malango
ya kifo.[q]
19 Nao wakaanza kumwomba
Yehova msaada katika
taabu yao;[r]
Na kutoka katika
mikazo iliyokuwa juu
yao akawaokoa kama
kawaida.[a]
20 Akatuma neno lake na
kuwaponya[b]
Na kuwaokoa kutoka
katika mashimo yao.[c]
21 Watu na wamshukuru
Yehova kwa ajili ya
fadhili zake zenye
upendo[d]
Na kwa ajili ya kazi zake
za ajabu kwa wana wa
binadamu.[e]
22 Na watoe dhabihu za kutoa
shukrani[f]
Na kutangaza kazi zake
kwa vigelegele vya
shangwe.[g]
23 Wale wanaoshuka baharini
kwa meli,[h]
Wanaofanya biashara
katika maji mengi,[i]
24 Hao ndio ambao
wameziona kazi za
Yehova[j]
Na kazi zake za ajabu
vilindini;[k]
25 Jinsi anavyosema neno na
kutokeza upepo wenye
tufani,[l]
Hivi kwamba unainua
mawimbi yake.[m]
26 Wao hupanda juu mbinguni,
Hushuka mpaka chini.
Kwa sababu ya msiba nafsi
yao hujikuta inayeyuka.[n]
27 Wanayumba-yumba na
kwenda huku na huku
kama mlevi,[o]
Na hata hekima yao yote
huvurugika.[p]
28 Nao huanza kumpaazia
Yehova kilio katika
taabu yao,[q]
Naye huwatoa katika
mikazo iliyo juu yao.[r]

SURA 107

a Omb 3:42
b Zb 106:43
c 2Nya 33:10
Zb 73:24
Met 1:25
Lu 7:30
d Law 26:21
Amu 10:15
Lu 15:17
e 2Fa 6:27
Zb 22:11
f Amu 4:3
Amu 6:6
Amu 10:10
2Nya 33:12
g Amu 10:12
h Zb 68:6
Isa 49:9
Efe 5:8
1Pe 2:9
i Zb 146:7
Isa 61:1
Mdo 12:7
Mdo 16:26
j Omb 3:22
k Zb 92:5
l Isa 45:1
m Isa 45:2
n Met 1:7
Omb 3:39
o Hes 11:33
Zb 38:5
Yer 2:19
Ga 6:7
2Pe 2:13
p Ayu 33:20
q Ayu 33:22
Ayu 38:17
Zb 9:13
Zb 88:3
Zb 116:3
Ufu 1:18
r Yer 33:3

Safu ya 2

a Zb 34:6
b Hes 21:8
2Fa 20:5
Zb 30:2
Zb 103:3
Zb 147:3
c Ayu 33:28
Zb 30:3
Zb 49:15
Zb 56:13
Zb 103:4
d Zb 138:2
e Zb 66:5
f Law 7:12
Zb 50:14
Zb 116:17
Ebr 13:15
1Pe 2:5
g Zb 9:11
Zb 73:28
Zb 118:17
h 1Fa 9:27
Eze 27:26
i 2Nya 9:21
Eze 27:9
Ufu 18:17
j Zb 95:5
k Mwa 1:21
Zb 104:25
l Zb 135:7
Zb 148:8
Yer 10:13
Yon 1:4
m Zb 93:4
n 2Sa 17:10
Zb 22:14
Isa 13:7
Nah 2:10
o Ayu 12:25
Isa 19:14

p Isa 19:3; Yon 1:5; q Yon 1:14; r Yon 2:10.

29 Huituliza dhoruba ya upepo ikawa kimya,[a]
Hivi kwamba mawimbi ya bahari hukaa kimya.[b]
30 Nao hushangilia kwa sababu yanatulia,
Naye huwapeleka kwenye bandari inayowapendeza.[c]
31 Watu na wamtolee Yehova shukrani kwa ajili ya fadhili zake zenye upendo[d]
Na kwa ajili ya kazi zake za ajabu kwa wana wa binadamu.[e]
32 Na wamtukuze katika kutaniko la watu;[f]
Na katika kikao cha wazee na wampe sifa.[g]
33 Yeye huigeuza mito iwe nyika,[h]
Na chemchemi za maji ziwe nchi yenye ukame,[i]
34 Nchi yenye kuzaa iwe nchi ya chumvi,[j]
Kwa sababu ya ubaya wa wale wanaokaa humo.
35 Huigeuza nyika iwe dimbwi la maji lenye matete,[k]
Na nchi ya eneo lisilo na maji iwe chemchemi za maji.[l]
36 Na huko huwafanya wenye njaa wakae,[m]
Hivi kwamba wanasimamisha imara jiji la kukaa.[n]
37 Nao hupanda mbegu viwanjani na kupanda mashamba ya mizabibu,[o]
Ili yapate kutokeza mimea yenye kutoa mazao.[p]
38 Naye huwabariki hivi kwamba wanakuwa wengi sana;[q]
Wala haachi ng'ombe wao wawe wachache.[a]
39 Tena wanakuwa wachache na kuchutama[b]
Kwa sababu ya kizuizi, msiba na huzuni.[c]
40 Anamwaga dharau juu ya watu wenye vyeo,[d]
Hivi kwamba anawafanya watange-tange katika mahali penye ukiwa, pasipo na njia.[e]
41 Lakini humlinda maskini kutokana na mateso[f]
Na kumgeuza kuwa familia nyingi kama kundi.[g]
42 Wanyoofu huona na kushangilia;[h]
Lakini ukosefu wote wa uadilifu utafunga kinywa chake.[i]
43 Ni nani mwenye hekima? Atayashika mambo hayo[j]
Na kukaza fikira zake kwa matendo ya Yehova ya fadhili zenye upendo.[k]

Wimbo. Muziki wa Daudi.

108 Ee Mungu, moyo wangu uko imara.[l]
Nitaimba na kupiga muziki,[m]
Naam, utukufu wangu.[n]
2 Amka, Ee kinanda; nawe pia, Ee kinubi.[o]
Nitayaamsha mapambazuko.[p]
3 Nitakusifu katikati ya vikundi vya watu, Ee Yehova;[q]
Nami nitakupigia muziki katikati ya vikundi vya mataifa[r]

SURA 107

a Zb 89:9; Yon 1:15
b Mwa 8:1; Zb 65:7
c Yoh 6:21
d Zb 50:23; Zb 86:13
e Zb 72:18; Zb 105:5; Ufu 15:3
f Zb 22:22; Zb 40:9; Zb 111:1
g Ayu 29:7; Mdo 4:8
h 1Fa 17:7; Isa 19:5; Isa 42:15
i 1Fa 18:5; Yer 14:3; Amo 4:7
j Mwa 13:10; Mwa 19:25; Kum 29:23
k Zb 114:8; Isa 35:7; Isa 41:18
l 2Fa 3:17
m Zb 146:7; Lu 1:53
n Zb 107:7
o Isa 65:21; Yer 29:5
p Mwa 26:12; Mdo 14:17
q Kut 1:7; Kum 7:13

Safu ya 2

a Mwa 30:43; Kum 7:14
b 1Sa 2:7
c Amu 6:3; 2Fa 10:32; 2Fa 13:7; 2Nya 15:5; Yer 51:34
d 1Fa 21:19; 2Fa 24:15; 2Fa 25:7
e Ayu 12:24
f 1Sa 2:8
g Zb 78:52
h Ayu 22:19; Zb 52:6; Zb 58:10
i Kut 11:7; Zb 63:11; Ro 3:19
j Kum 4:6; Zb 64:9; Met 1:5; Yer 9:12; Ho 14:9
k Zb 77:12; Zb 143:5; Yer 9:24

SURA 108

l Zb 57:7
m Zb 104:33; Mdo 16:25; Efe 5:19
n Zb 16:9
o Zb 33:2; Zb 81:2; Zb 149:3
p Zb 57:8
q Zb 138:1; Zb 145:12
r Zb 57:9

4 Kwa maana fadhili zako
zenye upendo ni kuu
mpaka mbinguni,[a]
Na ukweli wako mpaka
angani.[b]
5 Utukuzwe juu ya mbingu,
Ee Mungu;[c]
Na utukufu wako na uwe
juu ya dunia yote.[d]
6 Ili wapendwa wako
waokolewe,[e]
Ee, uokoe kwa mkono
wako wa kuume na
kunijibu.[f]
7 Mungu mwenyewe
amesema katika
utakatifu wake:[g]
"Nitashangilia,
nitamgawanya
Shekemu[h] awe fungu;[i]
Na nchi tambarare
ya chini ya Sukothi[j]
nitaipima.
8 Gileadi[k] ni yangu; Manase[l]
ni yangu;
Na Efraimu ni ngome ya
aliye mkuu wangu;[m]
Yuda ni fimbo yangu ya
kiongozi.[n]
9 Moabu[o] ni chungu changu
cha kuoshea.[p]
Nitatupa kiatu[q] changu
juu ya Edomu.[r]
Nitapiga kelele za ushindi[s]
juu ya Ufilisti."[t]
10 Ni nani atakayenipeleka
kwenye jiji lenye ngome?[u]
Ni nani ambaye kwa kweli
ataniongoza mpaka
Edomu?[v]
11 Je, si wewe, Ee Mungu
ambaye umetutupilia
mbali[w]
Na ambaye huendi pamoja
na majeshi yetu ukiwa
Mungu?[x]
12 Utusaidie kutokana na
taabu,[y]
Kwa maana wokovu wa
mtu wa udongo haufai
kitu.[a]
13 Mungu atatuwezesha
kupata nguvu,[b]
Na yeye mwenyewe
atawakanyagia chini
wapinzani wetu.[c]

Kwa kiongozi. Ya Daudi. Muziki.

109 Ee Mungu wa
sifa yangu,[d] usikae
kimya.[e]
2 Kwa maana kinywa cha
mwovu na kinywa cha
udanganyifu
vimefunguka juu yangu.[f]
Wamesema juu yangu kwa
ulimi wa uwongo;[g]
3 Na kwa maneno ya chuki
wamenizingira,[h]
Nao wanaendelea
kupigana nami bila
sababu.[i]
4 Wanaendelea kunipinga
kwa sababu ya upendo
wangu;[j]
Lakini kwangu kuna sala.[k]
5 Nao wananitendea mabaya
kwa yaliyo mema[l]
Na chuki kwa upendo
wangu.[m]
6 Mweke mtu mwovu juu
yake,
Na mpinzani[n] aendelee
kusimama kwenye
mkono wake wa kuume.
7 Anapohukumiwa, na
aende zake kama
mwovu;
Na sala yake na iwe
dhambi.[o]
8 Siku zake na ziwe chache;[p]
Cheo chake cha uangalizi
mtu mwingine na
akichukue.[q]

SURA 108

a Zb 36:5 Zb 57:10 Zb 103:11
b Zb 71:22
c Zb 8:1 Zb 57:5
d Zb 57:11
e Zb 60:5 2Ko 1:10
f Kut 6:6 Zb 20:6
g Zb 89:35
h Yos 17:7
i Zb 60:6
j Mwa 33:17 Amu 8:5
k Yos 13:11 2Sa 2:9
l Zb 80:2
m Kum 33:17 Zb 60:7
n Mwa 49:10
o 2Sa 8:2
p Zb 60:8
q 2Sa 8:14
r Hes 24:18
s 2Sa 21:18
t Kut 15:14 2Sa 21:15
u Zb 60:9
v 2Fa 14:7 Oba 3
w Zb 44:9
x Kum 23:14 Zb 60:10
y Zb 18:6 Zb 20:1

Safu ya 2

a Zb 60:11 Zb 118:8 Zb 146:3
b 1Sa 2:4 2Sa 22:40 Zb 18:32 Zb 84:7 Isa 40:29 2Ko 4:7 Flp 4:13
c Isa 25:10 Ro 16:20

SURA 109

d Kut 15:2 Zb 33:1 Zb 118:28
e Kum 10:21 Zb 83:1
f 2Sa 15:3 Zb 31:18 Met 15:28 Mt 26:59
g Met 6:17 Met 26:28 Yer 9:3
h 2Sa 16:7 Ho 11:12
i 2Sa 15:12 Zb 35:7 Zb 69:4 Yoh 15:25
j 2Sa 13:39 Zb 35:12
k Zb 55:16
l Zb 35:7 Zb 38:20 Met 17:13
m Zb 55:12
n 1Sa 29:4 2Sa 19:22 1Fa 11:14 Zek 3:1

o Met 15:29; Met 28:9; Isa 1:15; Mik 3:4; p Zb 55:23; Zb 69:25; Mt 27:5; Mdo 1:18; q Mdo 1:20.

9 Wanawe na wawe wavulana wasio na baba[a]
Na mke wake awe mjane.[b]
10 Na wanawe watange-tange;[c]
Nao waombe-ombe,
Nao watafute chakula kutoka katika mahali pao penye ukiwa.[d]
11 Mla-riba na aweke mitego kwa ajili ya vyote alivyo navyo,[e]
Na wageni[f] wapore mazao yake ya kazi ya taabu.[g]
12 Na akose mtu wa kumwonyesha fadhili zenye upendo,[h]
Wala kusiwe na mtu anayewaonyesha kibali wavulana wake wasio na baba.
13 Wazao wake na wakatiliwe mbali.[i]
Katika kizazi kinachofuata jina lao na lifutiliwe mbali.[j]
14 Kosa la mababu zao na likumbukwe na Yehova,[k]
Na dhambi ya mama yake[l]—isifutiliwe mbali.[m]
15 Na wawe mbele za Yehova daima;[n]
Naye akatilie mbali kumbukumbu lao kutoka duniani;[o]
16 Kwa sababu hakukumbuka kuonyesha fadhili zenye upendo,[p]
Bali aliendelea kumfuatilia mtu mwenye kuteseka na aliye maskini[q]
Na mwenye huzuni moyoni, ili kumuua.[r]
17 Naye aliendelea kuipenda laana,[s] hivi kwamba ikamjia;[t]
Wala hakupendezwa na baraka,[a]
Hivi kwamba ikawa mbali naye;[b]
18 Naye akavikwa laana kuwa vazi lake.[c]
Kwa hiyo ikaja kama maji katikati yake[d]
Na kama mafuta ndani ya mifupa yake.
19 Na iwe kwake kama vazi ambalo yeye huvaa[e]
Na kama mshipi ambao yeye huendelea kujifunga daima.[f]
20 Hayo ndiyo malipo yanayotoka kwa Yehova ya mtu anayenipinga[g]
Na ya wale wanaosema maovu juu ya nafsi yangu.[h]
21 Lakini wewe ni Yehova Bwana Mwenye Enzi Kuu.[i]
Nitendee kwa ajili ya jina lako.[j]
Kwa sababu fadhili zako zenye upendo ni njema, unikomboe.[k]
22 Kwa maana nateseka nami ni maskini,[l]
Na moyo wangu umechomwa ndani yangu.[m]
23 Kama wakati kivuli kinapopungua, mimi nalazimika kwenda zangu;[n]
Nimekung'utwa kama nzige.
24 Magoti yangu yametetemeka kwa sababu ya kufunga,[o]
Na mwili wangu umekonda, bila kuwa na mafuta yoyote.[p]
25 Na kwao mimi nimekuwa kitu cha kushutumiwa.[q]

SURA 109

a Kut 22:24
b Yer 18:21
c 2Fa 5:27
d 2Sa 3:29
e Ne 5:7
f Isa 1:7
g Kum 28:33
Kum 28:51
Amu 6:5
h Yak 2:13
i 1Sa 2:31
2Fa 10:11
Zb 37:28
Yer 22:30
j Kut 32:33
Hes 5:23
Kum 25:19
Kum 29:20
Met 10:7
k Kut 20:5
Law 26:39
2Sa 3:29
2Sa 21:1
Mt 23:32
l 2Nya 22:3
m Ne 4:5
Yer 18:23
n Kum 32:34
Yer 2:22
o Zb 34:16
Isa 65:15
p 2Sa 17:2
Mt 18:33
Yak 2:13
q Mwa 42:21
Zb 10:2
r 2Sa 16:11
Zb 34:18
Zb 37:32
s Met 26:2
t Kum 28:45
Met 14:14
Eze 35:6

Safu ya 2

a Kum 28:2
2Th 2:10
b Zb 119:150
c Zb 73:6
d Hes 5:22
Mdo 1:18
e 2Fa 3:3
Zb 109:29
f Ayu 12:21
Yer 13:11
g 2Sa 17:23
Ro 6:23
1Pe 1:17
h Mt 26:66
i Ufu 6:10
j Zb 25:11
Zb 31:3
Yoh 17:11
k Zb 36:7
Zb 69:16
Zb 86:5
l Zb 40:17
Zb 86:1
2Ko 8:9
m 2Fa 4:27
Zb 102:4
n 1Nya 29:15
Ayu 14:2
Zb 102:11
Zb 144:4
Yak 4:14
o Zb 69:10
p Ayu 19:20
q Zb 31:11
Ro 15:3
Ebr 13:13

Wananiona—wanaanza
kutikisa kichwa chao.[a]
26 Unisaidie, Ee Yehova
Mungu wangu;[b]
Uniokoe kulingana na
fadhili zako zenye
upendo.[c]
27 Na wapate kujua ya
kwamba huu ni mkono
wako;[d]
Kwamba ni wewe
mwenyewe, Ee Yehova,
ambaye umelitenda.[e]
28 Wao na watangaze laana,[f]
Lakini wewe utangaze
baraka.[g]
Wamesimama, lakini
acha waone aibu,[h]
Na mtumishi wako na
ashangilie.[i]
29 Wale wanaonipinga na
wavikwe fedheha,[j]
Na acha wavae wenyewe
aibu yao kana kwamba
ni koti lisilo na mikono.[k]
30 Nitamsifu sana Yehova
kwa kinywa changu,[l]
Na katikati ya watu wengi
nitamsifu.[m]
31 Kwa maana yeye
atasimama kwenye
mkono wa kuume wa
maskini,[n]
Ili amwokoe kutoka kwa
wale wanaoihukumu
nafsi yake.

Ya Daudi. Muziki.

110

Neno la Yehova kwa
Bwana wangu ni:[o]
"Keti kwenye mkono
wangu wa kuume[p]
Mpaka niwaweke adui
zako kuwa kiti cha
miguu yako."[q]
2 Yehova atatuma fimbo[r]
ya nguvu zako kutoka
Sayuni,[s] akisema:
"Nenda ukitiisha katikati
ya adui zako."[a]
3 Watu wako[b] watajitoa kwa
hiari[c] katika siku ya
jeshi lako.[d]
Katika fahari za
utakatifu,[e] kutoka
tumbo la uzazi la
mapambazuko,
Una kundi lako la vijana
kama matone ya
umande.[f]
4 Yehova ameapa[g] (naye
hatajuta):[h]
"Wewe ni kuhani mpaka
wakati usio na kipimo[i]
Kwa mfano wa
Melkizedeki!"[j]
5 Yehova mwenyewe akiwa
upande wako wa mkono
wa kuume[k]
Hakika atawavunja
vipande-vipande
wafalme katika siku ya
hasira yake.[l]
6 Atatekeleza hukumu
katikati ya mataifa;[m]
Atafanya maiti zijae.[n]
Hakika atamvunja
vipande-vipande aliye
kichwa juu ya nchi
yenye hesabu kubwa
ya watu.[o]
7 Kutoka katika bonde la
mto njiani atakunywa.[p]
Ndiyo sababu atakiinua
kichwa chake juu.[q]

111

Msifuni Yah![r]

ℵ [*'A'leph*]

Nitamsifu Yehova kwa
moyo wangu wote[s]

SURA 109

a Zb 22:7; Mt 27:39
b Zb 40:13; Zb 119:86
c Zb 69:16; Zb 85:7; Zb 119:41
d Kut 13:3; Ne 2:8
e Hes 16:30; 1Fa 18:36
f Hes 22:6; 2Sa 16:10
g Hes 23:20
h Isa 65:15
i Isa 65:13; Ebr 12:2
j Zb 109:20
k Zb 6:10; Zb 35:26; Zb 132:18
l Zb 7:17; Zb 9:1; Zb 51:15; Ebr 13:15
m Zb 22:22
n Zb 16:8; Zb 72:4; Zb 110:5; Zb 121:5

SURA 110

o Mt 22:43; Lu 20:42
p Mk 12:36; Mdo 2:34; Mdo 7:56; Ro 8:34; Efe 1:20; Kol 3:1; Ebr 1:3; Ebr 8:1; Ebr 10:12; Ebr 12:2; 1Pe 3:22
q Mt 22:44; Mdo 2:35; 1Ko 15:25; Ebr 1:13; Ebr 10:13
r Mt 28:18; Ufu 2:27; Ufu 12:5; Ufu 19:15
s Ufu 11:15; Ufu 14:1

Safu ya 2

a Zb 2:9; Zb 45:4; Zb 45:5; Mt 24:30; Lu 19:27; Ufu 1:7; Ufu 6:2; Ufu 11:18
b Ufu 14:4
c Amu 5:2; Zb 119:108; Isa 6:8; Mt 4:20; Lu 5:28; 1Ko 9:17
d Mt 24:37; Mt 25:31; Ufu 6:2; Ufu 19:11
e Da 12:10; 2Ko 7:1; 1Pe 1:16
f Mwa 27:28; Mdo 4:4; Ufu 7:9
g Ebr 6:13
h Hes 23:19; Ro 11:29; Ebr 7:20; **i** Ebr 7:21; Ebr 7:28; **j** Mwa 14:18; Zek 6:13; Ebr 5:6; Ebr 6:20; Ebr 7:3; Ebr 7:11; Ebr 7:17; **k** Zb 16:8; Zb 121:5; **l** Zb 2:2; Eze 38:18; Ro 2:5; Ufu 11:18; Ufu 19:19; **m** Zb 79:6; Zb 149:7; **n** Yer 25:33; 2Pe 3:10; **o** Mwa 3:15; Zb 68:21; Hab 3:13; **p** Amu 7:5; 1Fa 17:4; **q** Zb 3:3; Isa 53:12; **SURA 111** **r** Kut 15:2; Zb 35:18; Zb 68:4; Zb 113:1; Ufu 19:1; **s** Zb 9:1; Zb 107:8; Zb 138:1.

ב [*Behth*]

Katika kikundi cha rafiki za karibu[a] walio wanyoofu na katika kusanyiko.[b]

ג [*Gi'mel*]

2 Kazi za Yehova ni kuu,[c]

ד [*Da'leth*]

Zinazotafutwa na wale wote wanaopendezwa nazo.[d]

ה [*He'*]

3 Utendaji[e] wake ni utukufu na fahari,[f]

ו [*Waw*]

Na uadilifu wake unasimama milele.[g]

ז [*Za'yin*]

4 Amefanya ukumbusho kwa ajili ya kazi zake za ajabu.[h]

ח [*Chehth*]

Yehova ni mwenye neema na mwenye rehema.[i]

ט [*Tehth*]

5 Amewapa chakula wale wanaomwogopa.[j]

י [*Yohdh*]

Mpaka wakati usio na kipimo, atalikumbuka agano lake.[k]

כ [*Kaph*]

6 Nguvu za kazi zake amewatangazia watu wake,[l]

ל [*La'medh*]

Kwa kuwapa urithi wa mataifa.[m]

מ [*Mem*]

7 Kazi za mikono yake ni kweli na hukumu;[n]

נ [*Nun*]

Maagizo yake yote anayotoa ni yenye kutegemeka,[o]

SURA 111

a Ayu 19:19 Zb 89:7
b 1Fa 8:5 Zb 1:5
c Ayu 9:10 Ayu 42:2 Zb 92:5 Zb 98:1 Zb 104:24 Zb 139:14 Isa 40:12 Ufu 15:3
d Zb 77:12 Zb 92:4 Zb 143:5
e Kum 32:4 Zb 64:9
f Kut 15:6 1Nya 16:27 Ayu 40:10 Zb 145:12
g Zb 98:2 Zb 103:17 Isa 5:16
h Kum 31:19 Yos 4:7 Zb 102:12
i Kut 34:6 Zb 78:38 Zb 86:5 Zb 103:8 Yak 5:11
j Zb 34:9 Zb 37:25 Mt 6:33
k Ne 1:5 Zb 89:34 Zb 105:8
l Kum 4:32 Yos 6:20 Yos 10:13 Zb 78:12
m Zb 44:2 Zb 78:55 Zb 80:8 Zb 105:44
n Kum 32:4 Zb 85:10 Zb 86:8 Zb 98:3 Ufu 15:4
o Zb 19:8 Zb 33:4 Zb 119:4 Isa 55:11

Safu ya 2

a Zb 119:100 Isa 40:8
b Zb 19:9 Ufu 15:3
c Kut 15:13 Kum 15:15 Zb 130:7 Mt 1:21 Lu 1:68 Ufu 7:10
d 2Sa 23:5 1Nya 16:15 Yer 33:20
e Kum 28:58 1Nya 16:10 Zb 89:7 Zb 99:3 Isa 6:3 Mal 1:14 Lu 1:49 Ufu 4:8
f Kum 4:6 Ayu 28:28 Met 1:7 Met 9:10 Mhu 12:13 Ebr 11:7

ס [*Sa'mekh*]

8 Yanategemezwa vema milele, mpaka wakati usio na kipimo,[a]

ע [*'A'yin*]

Yanafanywa katika kweli na unyoofu.[b]

פ [*Pe'*]

9 Ameutuma ukombozi kwa watu wake.[c]

צ [*Tsa·dheh'*]

Mpaka wakati usio na kipimo ameamuru agano lake.[d]

ק [*Qohph*]

Jina lake ni takatifu na lenye kuogopesha.[e]

ר [*Rehsh*]

10 Kumwogopa Yehova ni mwanzo wa hekima.[f]

ש [*Sin*]

Wale wote wanaoyatenda maagizo yake wana ufahamu mwema.[g]

ת [*Taw*]

Sifa yake inasimama milele.[h]

112

Msifuni Yah![i]

א [*'A'leph*]

Mwenye furaha ni mtu anayemwogopa Yehova,[j]

ב [*Behth*]

Ambaye amependezwa[k] sana na amri zake.[l]

ג [*Gi'mel*]

2 Uzao wake utakuwa wenye nguvu duniani.[m]

ד [*Da'leth*]

Nacho kizazi cha wanyoofu, kitabarikiwa.[n]

---

g Kum 4:6; Yos 1:8; 1Fa 2:3; Met 3:4; 2Ti 3:15; **h** Zb 145:2; 1Pe 1:7; **SURA 112** **i** Kut 15:2; Zb 117:2; Zb 150:6; Ufu 19:1; **j** Zb 111:10; Zb 115:11; Zb 128:1; **k** Zb 1:2; Zb 40:8; Zb 119:16; Met 2:4; Ro 7:22; **l** Zb 119:6; **m** Zb 25:13; Zb 37:26; Zb 102:28; Mdo 2:39; **n** Mwa 17:7; Mwa 22:17; Zb 14:5; Zb 24:6.

ה [*He'*]

3 Vitu vyenye thamani na utajiri vimo nyumbani mwake;[a]

ו [*Waw*]

Nao uadilifu wake unasimama milele.[b]

ז [*Za'yin*]

4 Ameangaza katika giza kama nuru kwa walio wanyoofu.[c]

ח [*Chehth*]

Yeye ni mwenye neema na mwenye rehema na mwadilifu.[d]

ט [*Tehth*]

5 Mtu mwenye neema[e] na anayekopesha[f] ni mwema.

י [*Yohdh*]

Yeye hutegemeza mambo yake kwa haki.[g]

כ [*Kaph*]

6 Kwa kuwa hatatikiswa kamwe.[h]

ל [*La'medh*]

Mwadilifu atakuwa kumbukumbu mpaka wakati usio na kipimo.[i]

מ [*Mem*]

7 Hataogopa hata habari mbaya.[j]

נ [*Nun*]

Moyo wake ni imara,[k] umefanywa umtegemee Yehova.[l]

ס [*Sa'mekh*]

8 Moyo wake hauwezi kutikiswa;[m] hataogopa,[n]

ע [*'A'yin*]

Mpaka awatazame wapinzani wake.[o]

פ [*Pe'*]

9 Amegawa kwa wingi; amewapa maskini.[p]

SURA 112

a Zb 24:1 Isa 33:6 Mt 6:33
b Zb 111:3 Isa 32:17 Isa 51:8
c Zb 97:11 Isa 58:10 1Pe 2:9 1Yo 1:5 Ufu 22:5
d Ne 9:17 Mik 7:19 Lu 6:36 Efe 4:32 Kol 3:13
e Mdo 6:8
f Kum 15:8 Ayu 31:16 Zb 37:26 Zb 41:1 Met 14:21 Met 17:5 Met 19:17 Met 21:13 Lu 6:35 Lu 23:50 Mdo 20:35 Ebr 13:16
g 1Sa 12:3 Ayu 1:1 Mik 6:8 Mt 1:19 Efe 5:15 Kol 4:5 1Th 2:10
h Zb 15:5 Zb 125:1 Met 2:21 2Pe 1:10
i Ne 5:19 Met 10:7
j Zb 27:1 Met 1:33 Met 3:25 Lu 21:9
k Zb 57:7 Zb 118:6 Mdo 21:13
l Zb 62:8 Zb 64:10 Zb 118:8 Isa 26:3 Yoh 14:1 Mdo 27:25
m Zb 27:14 Zb 31:24
n Zb 56:11 Met 28:1
o Zb 59:10 Zb 91:8 Zb 92:11 Zb 118:7
p Kum 15:11 Met 11:24 Met 19:17 Mhu 11:2 2Ko 9:9

Safu ya 2

a Kum 24:13 Mt 25:46 Ebr 6:10
b 1Sa 2:1 Zb 75:10 Zb 92:10
c Est 6:11 Lu 13:28
d Zb 37:12 Zb 58:7
e Met 10:28 Met 11:7

צ [*Tsa·dheh'*]

Uadilifu wake unasimama milele.[a]

ק [*Qohph*]

Pembe yake mwenyewe itainuliwa kwa utukufu.[b]

ר [*Rehsh*]

10 Mwovu ataona na hakika atakasirika.[c]

ש [*Shin*]

Atasaga meno yake na kuyeyuka.[d]

ת [*Taw*]

Tamaa ya waovu itaangamia.[e]

113 Msifuni Yah![f]
Toeni sifa, enyi watumishi wa Yehova,[g]
Lisifuni jina la Yehova.[h]

2 Jina la Yehova na libarikiwe[i]
Kutoka sasa mpaka wakati usio na kipimo.[j]

3 Kutoka mapambazuko ya jua mpaka kutua kwake[k]
Jina la Yehova ni la kusifiwa.[l]

4 Yehova amekuwa juu ya mataifa yote;[m]
Utukufu wake uko juu ya mbingu.[n]

5 Ni nani aliye kama Yehova Mungu wetu,[o]
Yeye anayefanya makao yake juu?[p]

6 Yeye anajishusha kutazama mbingu na dunia,[q]

7 Akimwinua mtu wa hali ya chini kutoka kwenye mavumbi;[r]

SURA 113 **f** Kut 15:2; Zb 68:4; Zb 150:6; Isa 38:19; Ufu 19:1; **g** Zb 33:1; Zb 103:21; Efe 5:19; Ufu 19:5; **h** Zb 135:1; **i** 1Nya 29:10; Da 2:20; **j** 1Nya 16:36; Zb 106:48; **k** Isa 45:6; Isa 59:19; **l** Kut 9:16; Zb 72:19; Zb 86:9; Mal 1:11; **m** Zb 97:9; Zb 99:2; Isa 40:17; **n** 1Fa 8:27; Zb 8:1; **o** Kut 15:11; Zb 89:6; Isa 36:7; **p** 1Fa 8:43; Zb 11:4; Isa 57:15; Ebr 9:24; **q** Zb 14:2; Zb 18:35; Zb 102:19; Zb 138:6; Isa 66:2; **r** Zb 22:15.

Humwinua maskini
kutoka kwenye shimo la
majivu,[a]
8 Ili kumketisha pamoja na
wenye vyeo,[b]
Wenye vyeo kati ya watu
wake.[c]
9 Anampa mwanamke tasa
makao katika nyumba[d]
Kama mama ya wana aliye
na shangwe.[e]
Msifuni Yah![f]

114 Israeli alipotoka
Misri,[g]
Nyumba ya Yakobo
kutoka kwenye kikundi
cha watu wanaosema
maneno yasiyoeleweka,[h]
2 Yuda ikawa mahali pake
patakatifu,[i]
Israeli miliki yake kuu.[j]
3 Bahari iliona na
kukimbia;[k]
Yordani nao ulianza
kurudi nyuma.[l]
4 Milima ilirukaruka kama
kondoo-dume,[m]
Vilima kama wana-kondoo.
5 Ulikuwa na nini, Ee
bahari, hata ukakimbia,[n]
Ee Yordani, hata ukaanza
kurudi nyuma?[o]
6 Enyi milima, hata
mkarukaruka kama
kondoo-dume;[p]
Enyi vilima, kama
wana-kondoo?[q]
7 Kwa sababu ya Bwana uwe
na maumivu makali, Ee
dunia,[r]
Kwa sababu ya Mungu wa
Yakobo.
8 Ambaye anabadili
mwamba kuwa dimbwi
la maji lenye matete,[s]
Jiwe gumu kuwa bubujiko
la maji.[a]

115 Sisi hatuna chochote,
Ee Yehova, sisi
hatuna chochote,[b]
Bali jina lako ulitukuze[c]
Kulingana na fadhili zako
zenye upendo, kulingana
na ukweli wako.[d]
2 Kwa nini mataifa yaseme:[e]
"Yuko wapi, sasa, Mungu
wao?"[f]
3 Lakini Mungu wetu yuko
mbinguni;[g]
Kila kitu ambacho
alipendezwa kufanya,
amekifanya.[h]
4 Sanamu zao ni fedha na
dhahabu,[i]
Kazi ya mikono ya mtu wa
udongo.[j]
5 Zina kinywa, lakini
haziwezi kusema;[k]
Zina macho, lakini
haziwezi kuona;[l]
6 Zina masikio, lakini
haziwezi kusikia.[m]
Zina pua, lakini haziwezi
kunusa.[n]
7 Zina mikono, lakini
haziwezi kugusa.[o]
Zina miguu, lakini
haziwezi kutembea;[p]
Hazitoi sauti yoyote kwa
koo zao.[q]
8 Wale wanaozifanya
watakuwa kama hizo,[r]
Wale wote
wanaozitegemea.[s]
9 Ee Israeli, mtegemeeni
Yehova;[t]

SURA 113

a 1Sa 2:7
2Sa 7:8
Ayu 2:8
Flp 2:9
b Mwa 41:41
Ayu 36:7
c Ufu 5:10
d 1Sa 2:5
Zb 68:6
e Isa 54:1
Ga 4:27
f Zb 112:1
Zb 117:1

SURA 114

g Kut 12:41
Kut 13:3
h Mwa 42:23
Zb 81:5
i Mwa 49:10
Zb 76:1
Zb 78:68
j Kut 6:7
Kut 19:6
Kut 25:8
Kut 29:45
Kum 27:9
Kum 32:9
k Kut 14:21
Zb 77:16
Zb 106:9
1Ko 10:1
l Yos 3:16
Zb 74:15
m Kut 19:18
Kut 20:18
Amu 5:4
Zb 29:6
Zb 68:8
Yer 4:24
Hab 3:6
n Kut 15:8
Yos 2:10
Hab 3:8
o Yos 4:23
p Isa 64:3
q Mik 6:1
Nah 1:5
r 1Nya 16:30
Ayu 9:6
Zb 77:18
Zb 97:4
s Kut 17:6
Hes 20:11
Zb 107:35

Safu ya 2

a Kum 8:15
Ne 9:15
1Ko 10:4

SURA 115

b Ayu 1:21
1Ti 6:7
c Kum 28:58
Isa 48:11
Eze 39:13
Yoh 12:28
d Zb 61:7
Zb 66:20
Zb 89:1
Zb 138:2
Mik 7:20
Ro 3:4
e Kut 32:12
Hes 14:15
Kum 32:27
f Zb 42:3
Zb 79:10
Yoe 2:17

g Zb 2:4; Zb 33:14; Zb 123:1; Isa 63:15; Mt 6:9; h Zb 135:6; Isa 46:10; Da 4:35; Ro 9:19; i Zb 97:7; Zb 135:15; Isa 46:6; Yer 10:9; j Kum 4:28; Isa 40:19; Isa 44:17; Yer 10:3; Mdo 19:26; k Hab 2:19; l Zb 135:16; m Zb 135:17; n 1Ko 10:19; o 1Sa 5:4; p 1Sa 5:3; Isa 46:7; Mdo 17:29; q Hab 2:18; r Zb 135:18; Isa 44:9; Ufu 9:20; s 2Fa 21:21; Zb 97:7; Yon 2:8; t 1Nya 5:20; Zb 32:10; Zb 62:8; Met 3:5.

Yeye ndiye msaada wao na
ngao yao.[a]
10 Ee nyumba ya Haruni,
mtegemeeni Yehova;[b]
Yeye ndiye msaada wao
na ngao yao.[c]
11 Ninyi mnaomwogopa
Yehova, mtegemeeni
Yehova;[d]
Yeye ndiye msaada wao
na ngao yao.[e]
12 Yehova mwenyewe
ametukumbuka; atatoa
baraka,[f]
Ataibariki nyumba ya
Israeli,[g]
Ataibariki nyumba ya
Haruni.[h]
13 Atawabariki wale
wanaomwogopa Yehova,[i]
Wadogo kwa wakubwa.[j]
14 Yehova atawapa ninyi
ongezeko,[k]
Ninyi na wana wenu.[l]
15 Ninyi ndio mliobarikiwa
na Yehova,[m]
Mtengenezaji wa mbingu
na dunia.[n]
16 Mbingu ni mbingu za
Yehova,[o]
Bali dunia amewapa wana
wa binadamu.[p]
17 Wafu wenyewe hawamsifu
Yah,[q]
Wala wowote wanaoingia
mahali penye
kimya.[r]
18 Lakini sisi wenyewe
tutambariki Yah[s]
Kutoka sasa mpaka
wakati usio na kipimo.[t]
Msifuni Yah![u]

116 Ninajawa na upendo,
kwa sababu Yehova
husikia[v]
Sauti yangu, kusihi
kwangu.[w]
2 Kwa maana yeye
amenitegea sikio lake,[a]
Nami nitaita siku zangu
zote.[b]
3 Kamba za kifo
zilinizunguka[c]
Na hali zenye kutaabisha
za Kaburi* zikanipata.[d]
Nikaendelea kupata taabu
na huzuni.[e]
4 Lakini nikaliitia jina la
Yehova:[f]
"Ah, Yehova, uiokoe nafsi
yangu!"[g]
5 Yehova ni mwenye neema
na ni mwadilifu;[h]
Naye Mungu wetu, Yeye
ni mwenye kuonyesha
rehema.[i]
6 Yehova anawalinda wasio
na uzoefu.[j]
Nilikuwa maskini, naye
akaniokoa.[k]
7 Rudi mahali pako pa
kupumzika, Ee nafsi
yangu,[l]
Kwa maana Yehova
mwenyewe amekutendea
inavyofaa.[m]
8 Kwa maana umeiokoa
nafsi yangu kutokana na
kifo,[n]
Jicho langu kutokana na
machozi, mguu wangu
kutokana na kujikwaa.[o]
9 Nitatembea[p] mbele za
Yehova katika nchi za
walio hai.[q]
10 Nilikuwa na imani,[r] kwa
maana nilisema.[s]
Mimi mwenyewe nilikuwa
nimeteseka sana.

SURA 115

a Kum 33:29; Zb 33:20; Zb 119:114; Zb 144:2; Met 30:5
b Kut 28:1; Kum 33:8
c Zb 118:3
d Met 16:20; Yer 17:7
e Zb 84:11
f Zb 136:23; Met 10:22; Mdo 10:4
g Mwa 12:2; Zb 67:7; Mdo 3:26
h Zb 115:10
i Zb 29:11; Lu 1:50; Mdo 13:26
j Mdo 26:22; Ufu 11:18; Ufu 19:5
k Mwa 13:16; Mwa 49:25
l Mwa 22:17
m Zb 3:8; Efe 1:3
n Mwa 1:1; Mwa 14:19; Zb 96:5; Zb 146:6
o Zb 89:11; Isa 66:1
p Mwa 1:28; Kum 32:8; Zb 37:29; Isa 45:18; Yer 27:5; Mdo 17:26
q Zb 6:5; Zb 30:9; Zb 118:17; Mhu 9:5; Isa 38:18
r 1Sa 2:9; Zb 31:17
s 1Nya 29:20; Zb 68:4
t Zb 113:2; Da 2:20
u Zb 112:1; Ufu 19:3

SURA 116

v Zb 18:6; Zb 66:19
w Da 9:3

Safu ya 2

a Zb 34:15
b Ne 2:4; Ayu 27:10
c Zb 18:4
d Isa 38:10
e Zb 38:6; Isa 53:3
f 2Nya 33:13; Zb 34:6; Ro 10:13
g Zb 41:1; Zb 89:48; Zb 118:25
h Kut 34:6; Kum 32:4; Ne 9:8; Zb 103:8; Zb 119:137; Zb 145:17; Ro 3:25
i Kut 20:6; Ne 9:17; Da 9:9
j Zb 19:7
k Zb 79:8; Zb 106:43; Zb 142:6; l Yer 6:16; m Zb 13:6; Zb 119:17; Zb 145:20; Ebr 11:6; n Zb 56:13; Zb 86:13; o 1Sa 25:34; Zb 94:18; p Mwa 17:1; Lu 1:6; q Zb 27:13; Zb 142:5; Mhu 9:5; Isa 38:11; Isa 53:8; r Mwa 15:6; 2Ko 4:13; Ebr 11:1; s Ro 10:10; 2Pe 1:21.

Zb 116:3* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

11 Mimi mwenyewe nilisema,
wakati nilipokuwa na wasiwasi mkubwa:[a]
"Kila mwanadamu ni mwongo."[b]
12 Nitamlipa Yehova nini[c]
Kwa ajili ya faida zake zote kwangu?[d]
13 Nitakichukua kikombe cha wokovu mkuu,[e]
Nami nitaliitia jina la Yehova.[f]
14 Nadhiri zangu nitamtimizia Yehova,[g]
Naam, mbele ya watu wake wote.
15 Ni chenye thamani machoni pa Yehova
Kifo cha washikamanifu wake.[h]
16 Ah, sasa, Ee Yehova,[i]
Kwa maana mimi ni mtumishi wako.[j]
Mimi ni mtumishi wako, mwana wa kijakazi wako.[k]
Umezifungua pingu zangu.[l]
17 Nitakutolea wewe dhabihu ya kutoa shukrani,[m]
Nami nitaliitia jina la Yehova.[n]
18 Nadhiri zangu nitamtimizia Yehova,[o]
Naam, mbele ya watu wake wote,[p]
19 Katika nyua za nyumba ya Yehova,[q]
Katikati yako, Ee Yerusalemu.[r]
Msifuni Yah![s]

117 Msifuni Yehova, enyi mataifa yote;[t]
Mtukuzeni, enyi jamii zote.[u]
2 Kwa maana fadhili zake zenye upendo zimekuwa zenye nguvu kwetu sisi;[v]
Na ukweli[a] wa Yehova ni wa mpaka wakati usio na kipimo.
Msifuni Yah![b]

118 Mshukuruni Yehova, kwa maana yeye ni mwema;[c]
Kwa maana fadhili zake zenye upendo ni za mpaka wakati usio na kipimo.[d]
2 Israeli na aseme sasa:
"Kwa maana fadhili zake zenye upendo ni za mpaka wakati usio na kipimo."[e]
3 Wale wa nyumba ya Haruni na waseme sasa:[f]
"Kwa maana fadhili zake zenye upendo ni za mpaka wakati usio na kipimo."[g]
4 Wale wanaomwogopa Yehova na waseme sasa:[h]
"Kwa maana fadhili zake zenye upendo ni za mpaka wakati usio na kipimo."[i]
5 Kutoka katika hali zenye kutaabisha nilimwitia Yah;[j]
Yah akanijibu na kuniweka katika mahali penye nafasi pana.[k]
6 Yehova yuko upande wangu; sitaogopa.[l]
Mtu wa udongo anaweza kunitenda nini?[m]
7 Yehova yuko upande wangu kati ya wale wanaonisaidia,[n]
Hivi kwamba mimi nitawatazama wale wanaonichukia.[o]

SURA 116

a Zb 31:22
b Zb 146:3 Ro 3:4
c Zb 50:10 1Ko 6:20
d Zb 103:2
e Zb 119:155
f Zb 150:1 Yoe 2:32 Mt 26:42
g Ayu 22:27 Zb 22:25 Yon 2:9
Nah 1:15 Mt 5:33 Yoh 17:4
h 1Sa 25:29 Ayu 1:12 Zb 50:5 Zb 72:14 Zb 91:14 Zek 2:8 2Pe 2:9
i Zb 116:4
j Zb 119:125 Zb 143:12
k Zb 86:16 Lu 1:38
l 2Nya 33:13 Zb 107:14
m Law 7:12 Zb 50:23 Zb 107:22 Ebr 13:15
n Ro 10:13
o Zb 22:25 Zb 76:11 Mhu 5:5
p Zb 116:14
q Zb 96:8 Zb 100:4 Zb 135:2
r Zb 122:3
s Zb 112:1 Ufu 19:1

SURA 117

t Zb 18:49 Zb 113:1 Ro 15:11 Ufu 7:10 Ufu 19:6
u Mwa 25:16 Hes 25:15
v Zb 94:18 Zb 100:5 Omb 3:22

Safu ya 2

a Zb 25:10 Zb 71:22 Zb 91:4 Isa 10:20 Lu 1:55
b Zb 111:1

SURA 118

c 1Nya 16:8 Zb 107:1 Mt 19:17
d Zb 136:1
e Zb 136:2
f Zb 135:19 1Pe 2:5
g Zb 136:3
h Zb 22:23 Ufu 19:5
i Zb 136:4
j Zb 50:15 Zb 107:19 Zb 120:1
k Kut 15:2 Zb 18:19
l Zb 27:1; Zb 146:5; Isa 51:12; Ro 8:31; m Zb 56:4; Ebr 13:6; n 1Nya 12:18; Zb 54:4; Mt 26:53; o Zb 54:7.

8 Ni afadhali kupata
kimbilio katika Yehova[a]
Kuliko kumtegemea mtu
wa udongo.[b]
9 Ni afadhali kupata
kimbilio katika Yehova[c]
Kuliko kuwategemea watu
wenye vyeo.[d]
10 Mataifa yote yalinizunguka.[e]
Nami niliendelea
kuwazuilia mbali katika
jina la Yehova.[f]
11 Walinizingira, naam,
walikuwa
wamenizingira.[g]
Nami niliendelea
kuwazuilia mbali katika
jina la Yehova.
12 Walinizunguka kama nyuki;[h]
Walizimwa kama moto wa
vichaka vya miiba.[i]
Nami niliendelea
kuwazuilia mbali katika
jina la Yehova.[j]
13 Ulinisukuma kwa nguvu
ili nianguke,[k]
Lakini Yehova mwenyewe
alinisaidia.[l]
14 Yah ni kinga yangu na
nguvu zangu,[m]
Naye huwa wokovu
kwangu.[n]
15 Sauti ya vigelegele vya
shangwe na wokovu[o]
Imo katika mahema[p] ya
waadilifu.[q]
Mkono wa kuume wa
Yehova unaonyesha
nguvu.[r]
16 Mkono wa kuume wa
Yehova unajiinua;[s]
Mkono wa kuume
wa Yehova unaonyesha
nguvu.[t]
17 Sitakufa, bali nitaendelea
kuishi,[u]
Ili nizitangaze kazi za Yah.[v]
18 Yah alinirekebisha vikali,[a]
Lakini hakunitia mikononi
mwa kifo.[b]
19 Nifungulieni malango ya
uadilifu.[c]
Mimi nitayaingia;
nitamsifu Yah.[d]
20 Hili ndilo lango la Yehova.[e]
Waadilifu wataliingia.[f]
21 Nitakusifu, kwa maana
ulinijibu[g]
Nawe ukawa wokovu
wangu.[h]
22 Jiwe ambalo wajenzi
walilikataa[i]
Limekuwa jiwe kuu la
pembeni.[j]
23 Hili limetokana na Yehova
mwenyewe;[k]
Ni la ajabu machoni petu.[l]
24 Hii ndiyo siku ambayo
Yehova ameifanya;[m]
Tutaishangilia na
kuifurahia.[n]
25 Ah, sasa, Yehova, uokoe,
tafadhali![o]
Ah, sasa, Yehova,
ufanikishe, tafadhali![p]
26 Na abarikiwe Yeye
anayekuja katika jina la
Yehova;[q]
Tumewabariki ninyi watu
kutoka katika nyumba
ya Yehova.[r]
27 Yehova ndiye Mungu,[s]
Naye hutupa nuru.[t]
Fungeni maandamano
ya sherehe[u] kwa
matawi,[v]
Mpaka kwenye pembe za
madhabahu.[w]
28 Wewe ni Mungu wangu,
nami nitakusifu;[x]

SURA 118

a Zb 40:4 Zb 62:8 Yer 17:5
b Zb 146:3
c Met 18:10
d Isa 30:2 Eze 29:7
e Zb 2:2 Zek 12:3
f 2Nya 20:17
g Zb 22:12
h Kum 1:44
i Zb 83:14 Mhu 7:6 Isa 27:4 Nah 1:10
j 2Nya 14:11
k 1Sa 20:3 Zb 18:18 Mik 7:8 Lu 4:29
l Mdo 2:32
m Kut 15:2 Zb 18:2 Isa 12:2
n Zb 3:8 Mdo 3:15
o Zb 30:11 Lu 24:52
p Isa 16:5
q Isa 65:13 Mdo 2:46 Mdo 16:34
r Zb 89:13 Isa 63:12
s Kut 15:6
t Isa 40:26
u Zb 6:5
v Zb 71:17 Zb 73:28

Safu ya 2

a Zb 66:10 Zb 94:12 Isa 53:10 2Ko 6:9 Ebr 12:6
b Zb 16:10 Mdo 2:31
c Isa 26:2 Mt 7:14 Ufu 22:14
d Kut 15:2
e Zb 24:7
f Zb 24:4 Isa 35:8
g Yoh 11:41
h Zb 116:1 Isa 12:2
i Isa 53:3 Mk 12:10 Lu 20:17 1Pe 2:4
j Isa 28:16 Zek 4:7 Lu 20:17 Mdo 4:11 1Ko 3:11 Efe 2:20 1Pe 2:6
k Mdo 3:15 Mdo 5:31
l Mk 12:11
m Zb 69:13 Zek 3:9 2Ko 6:2
n 1Fa 8:66 Est 8:16 Yoh 16:22 Mdo 5:41
o Zb 20:9 1Ti 2:3
p Zb 90:17

q Mt 21:9; Mt 23:39; Mk 11:9; Lu 19:38; r Zb 134:3; s Yos 22:22; Zb 50:1; Isa 46:9; t Zb 18:28; 1Pe 2:9; u Zb 42:4; v Law 23:34; Mt 21:8; Yoh 12:13; Ufu 7:9; w Kut 27:2; x Kut 15:2; Isa 25:1.

Mungu wangu—
nitakutukuza.[a]
29 Mshukuruni Yehova, kwa
maana yeye ni mwema;[b]
Kwa maana fadhili zake
zenye upendo ni za
mpaka wakati usio na
kipimo.[c]

א [*A'leph*]

119 Wenye furaha ni
wale wasio na kosa
katika njia yao,[d]
Wale wanaotembea katika
sheria ya Yehova.[e]
2 Wenye furaha ni
wale wanaoshika
vikumbusho vyake;[f]
Wanaendelea kumtafuta
kwa moyo wote.[g]
3 Kwa kweli hawakuzoea
kufanya ukosefu
wowote wa uadilifu.[h]
Wametembea katika njia
zake.[i]
4 Wewe mwenyewe umetoa
maagizo yako kwa
kuamuru[j]
Yashikwe kwa uangalifu.[k]
5 Laiti njia zangu
zingefanywa imara[l]
Ili kushika masharti
yako![m]
6 Ndipo singeona aibu,[n]
Ninapozitazama amri
zako zote.[o]
7 Nitakusifu katika
unyoofu wa moyo,[p]
Ninapojifunza maamuzi
yako ya hukumu yaliyo
ya uadilifu.[q]
8 Ninaendelea kushika
masharti yako.[r]
Ee, usiniache kabisa.[s]

ב [*Behth*]

9 Kijana[t] ataisafishaje njia
yake?
Kwa kujilinda kulingana
na neno lako.[u]
10 Nimekutafuta kwa moyo
wangu wote.[a]
Usinipotoshe niache amri
zako.[b]
11 Moyoni mwangu
nimeweka hazina ya
maneno yako,[c]
Ili nisikutendee dhambi.[d]
12 Umebarikiwa, Ee Yehova.
Unifundishe masharti
yako.[e]
13 Kwa midomo yangu
nimetangaza[f]
Maamuzi yote ya hukumu
ya kinywa chako.[g]
14 Nimeshangilia katika njia
ya vikumbusho vyako,[h]
Kama vile katika mambo
mengine yote yenye
thamani.[i]
15 Nitajishughulisha na
maagizo yako,[j]
Nami nitayatazama
mapito yako.[k]
16 Nitazipenda sheria zako.[l]
Sitalisahau neno lako.[m]

ג [*Gi'mel*]

17 Umtendee mtumishi
wako inavyofaa, ili
nipate kuishi[n]
Na ili nipate kulishika
neno lako.[o]
18 Ufunue macho yangu, ili
nipate kutazama[p]
Mambo ya ajabu kutoka
katika sheria yako.[q]
19 Mimi ni mkaaji mgeni tu
katika nchi.[r]
Usinifiche amri zako.[s]
20 Nafsi yangu imepondeka
kwa kutamani[t]
Maamuzi yako ya
hukumu wakati wote.[u]

SURA 118

a Zb 145:1
Isa 12:2
b Zb 50:23
c Ezr 3:11
Zb 118:1

SURA 119

d 2Fa 20:3
Ayu 1:1
Zb 32:2
Yak 5:11
e Zb 119:97
Zb 128:1
Ro 7:22
Yak 1:25
f Zb 19:7
Zb 119:157
g Kum 4:29
1Fa 8:48
1Nya 22:19
2Nya 31:21
Yer 29:13
h 2Sa 22:21
Yoh 7:18
Ro 10:5
1Yo 3:9
i Mwa 5:22
1Fa 2:3
2Nya 31:21
Isa 38:3
j Kum 5:33
Yer 7:23
Yoh 14:21
k Yak 2:10
1Yo 5:3
l Zb 51:10
m Kum 4:1
Zb 119:135
Yer 32:11
n Zb 119:80
o Law 27:34
Mhu 12:13
p 1Nya 29:17
q Kum 1:35
Kum 4:3
Kum 5:1
Kum 6:1
Zb 19:9
Zb 119:160
r Kum 4:1
Yos 24:15
Zb 119:145
s Zb 37:25
Isa 43:2
Ebr 13:5
t Zb 25:7
u Zb 15:2
Met 6:22

Safu ya 2

a 1Sa 7:3
2Nya 15:15
b Zb 25:5
Zb 119:118
c Zb 112:1
Zb 119:67
Lu 2:19
Lu 2:51
Ro 6:17
d Zb 19:13
Zb 37:31
e Ne 10:29
Zb 119:26
Zb 119:64
f Zb 40:9
g Hes 16:5
Kum 5:31
1Nya 16:12
Zb 19:9
h Zb 119:111
Yer 15:16
i Ayu 23:12
Zb 19:10
Zb 119:72

j Zb 19:8; Zb 111:7; Zb 119:93; Zb 119:100; Zb 119:173; k Zb 25:10; l Mwa 26:5; Kum 30:10; m Kum 4:13; Yoh 17:6; Yak 1:23; n Law 18:5; Zb 116:7; Isa 38:20; Ro 10:5; o Zb 119:110; 1Th 2:13; p 2Ko 3:18; q Ro 15:4; Ebr 8:5; Ebr 10:1; r Mwa 47:9; 1Nya 29:15; 1Pe 2:11; s Law 27:34; Hes 36:13; Zb 19:8; Zb 119:151; Mhu 12:13; t Zb 42:1; Zb 63:1; u Kum 1:35; Kum 6:20; Zb 105:5.

21 Umewakemea wenye
kimbelembele
waliolaaniwa,[a]
Ambao wanaziacha amri
zako.[b]
22 Niondolee shutuma na
dharau,[c]
Kwa maana nimeshika
vikumbusho vyako.[d]
23 Hata wakuu wameketi;
Wamesemezana dhidi
yangu.[e]
Naye mtumishi wako,
anajishughulisha na
masharti yako.[f]
24 Pia, ninavipenda
vikumbusho vyako,[g]
Ni kama wanaume wa
shauri langu.[h]

ד [*Da'leth*]

25 Nafsi yangu imekuwa
ikishikamana na
mavumbi.[i]
Nihifadhi hai kulingana
na neno lako.[j]
26 Nimezitangaza njia
zangu mwenyewe, ili
unijibu.[k]
Unifundishe masharti
yako.[l]
27 Unifanye nielewe njia
ya maagizo yako
mwenyewe,[m]
Ili nipate kujishughulisha
na kazi zako za ajabu.[n]
28 Nafsi yangu imekosa
usingizi kwa sababu ya
huzuni.[o]
Uniinue kulingana na
neno lako.[p]
29 Uniondolee njia ya
uwongo,[q]
Na kunipa kibali kwa
sheria yako.[r]
30 Nimeichagua njia ya
uaminifu.[s]
Nimeyaona maamuzi yako
ya hukumu kuwa yenye
kufaa.[t]

SURA 119

a Mal 4:1
1Pe 5:5
b Kum 28:15
Yer 11:3
c Yos 5:9
1Sa 25:39
Zb 123:3
d Zb 19:7
Zb 93:5
Zb 119:167
e 1Sa 20:31
Zb 2:2
Lu 22:66
f Kum 4:5
Zb 119:171
g Zb 19:7
Zb 119:14
Zb 119:168
h Kum 17:18
Zb 119:105
Met 1:25
2Ti 3:16
i Zb 22:15
Zb 44:25
j 2Sa 7:28
Zb 71:20
Zb 119:154
Zb 143:11
k 2Nya 32:20
Zb 38:18
Met 28:13
Isa 38:3
l Kum 4:5
1Fa 8:36
Zb 86:11
Isa 30:20
m Zb 103:18
Zb 119:94
n 1Nya 16:9
2Nya 32:22
Zb 105:2
Zb 145:5
o Zb 107:6
Isa 38:10
p Isa 38:20
Ho 6:2
q Zb 119:104
Zb 141:4
Met 30:8
Efe 4:25
r Ebr 8:10
s Yos 24:15
Met 12:22
Met 28:20
1Ko 4:2
t Law 18:5
Kum 4:3

Safu ya 2

a Zb 19:7
2Pe 3:1
b Zb 25:20
Zb 119:80
c Kum 30:16
d 1Fa 4:29
2Nya 30:19
2Ko 6:11
e Zb 119:64
Isa 48:17
Yoh 6:45
Yak 1:5
f Zb 119:112
Ufu 2:26
g Zb 19:7
Zb 105:45
Zb 119:1
h Zb 119:69
Kol 3:23
i Zb 19:8
Zb 23:3
Flp 2:13
j Zb 40:8
k Zb 119:119
Yer 44:23

31 Nimeshikamana na
vikumbusho vyako.[a]
Ee Yehova, usiniaibishe.[b]
32 Nitakimbia kwenye njia
ya amri zako,[c]
Kwa sababu wewe
huufanya moyo wangu
upate nafasi.[d]

ה [*He'*]

33 Unifundishe, Ee Yehova,
njia ya masharti yako,[e]
Ili nipate kuishika hata ile
ya mwisho.[f]
34 Unifanye nielewe, ili
nipate kuishika sheria
yako[g]
Nami nipate kuishika kwa
moyo wote.[h]
35 Unitembeze katika njia
ya amri zako,[i]
Kwa maana
nimependezwa nayo.[j]
36 Uelekeze moyo wangu
kwa vikumbusho
vyako,[k]
Wala si kwa faida.[l]
37 Uyafanye macho yangu
yapite ili yasione jambo
lisilofaa;[m]
Unihifadhi hai katika njia
yako mwenyewe.[n]
38 Umtimizie mtumishi
wako maneno yako[o]
Ambayo yanamwelekeza
kukuogopa wewe.[p]
39 Ufanye shutuma yangu
ipitilie mbali, ambayo
nimeiogopa,[q]
Kwa maana maamuzi
yako ya hukumu ni
mema.[r]
40 Tazama! nimeyatamani
maagizo yako.[s]
Unihifadhi hai katika
uadilifu wako.[t]

l Kut 18:21; Lu 12:15; 1Ti 6:10; Ebr 13:5; Yak 4:13; **m** Hes 15:39; Met 4:25; Met 23:5; Mt 7:17; **n** Zb 119:25; Isa 38:21; **o** 2Sa 7:25; **p** Zb 145:19; **q** Zb 39:8; **r** Kum 4:8; Zb 19:9; Zb 119:75; **s** Zb 19:8; Zb 119:15; **t** Zb 143:11.

ו [*Waw*]

41 Na fadhili zako zenye
upendo na zinijie, Ee
Yehova,[a]
Wokovu wako kulingana
na maneno yako,[b]
42 Nipate kumjibu yeye
anayenishutumu kwa
neno,[c]
Kwa maana
nimelitegemea neno
lako.[d]
43 Wala usiondoe kabisa
neno la kweli kutoka
kinywani mwangu,[e]
Kwa maana nimengojea
uamuzi wako
mwenyewe wa hukumu.[f]
44 Nami nitaishika sheria
yako daima,[g]
Mpaka wakati usio na
kipimo, naam, milele.[h]
45 Nami nitatembea huku
na huku katika mahali
penye nafasi tele,[i]
Kwa maana nimeyatafuta
maagizo yako.[j]
46 Pia nitasema juu
ya vikumbusho vyako
mbele ya wafalme,[k]
Wala sitaona aibu.[l]
47 Nami nitapendezwa na
amri zako[m]
Ambazo nimezipenda.[n]
48 Nami nitainua mikono
yangu kwenye amri
zako ambazo
nimezipenda,[o]
Nami nitajishughulisha
mwenyewe na masharti
yako.[p]

ז [*Za′yin*]

49 Ulikumbuke neno lako
kwa mtumishi wako,[q]
Ambalo umenifanya
nilingojee.[r]
50 Hii ndiyo faraja yangu
katika mateso yangu,[s]
Kwa maana maneno yako
mwenyewe
yamenihifadhi hai.[a]
51 Wenye kimbelembele
wamenidharau
kupindukia.[b]
Sijageuka kando kutoka
kwenye sheria yako.[c]
52 Nimeyakumbuka
maamuzi yako ya
hukumu tangu wakati
usio na kipimo, Ee
Yehova,[d]
Nami najipatia faraja.[e]
53 Hasira inayowaka
imenishika kwa sababu
ya waovu,[f]
Wanaoiacha sheria yako.[g]
54 Masharti yako yamekuwa
muziki kwangu[h]
Katika nyumba ya makao
yangu ya kigeni.[i]
55 Nimekumbuka jina lako
usiku, Ee Yehova,[j]
Ili nipate kuishika sheria
yako.[k]
56 Yote hayo yamekuwa
yangu,
Kwa sababu nimeyashika
maagizo yako.[l]

ח [*Chehth*]

57 Yehova ni fungu langu;[m]
Nimeahidi kuyashika
maneno yako.[n]
58 Nimeutuliza uso wako
kwa moyo wangu
wote.[o]
Unionyeshe kibali
kulingana na maneno
yako.[p]
59 Nimezifikiria njia zangu,[q]
Ili nipate kuirudisha
miguu yangu kwenye
vikumbusho vyako.[r]
60 Nilifanya haraka, nami
sikukawia[s]
Kuzishika amri zako.[t]

SURA 119

a Zb 51:1
Zb 85:7
Zb 90:14
Zb 106:4
Zb 119:76
b Mwa 49:18
Zb 14:7
Lu 2:30
c Mt 4:4
Mt 10:19
d Zb 119:49
Zb 119:81
Zb 119:105
e Zb 50:16
Zb 71:18
Isa 59:21
f Hes 16:5
Zb 19:9
g Zb 19:7
Zb 119:1
Zb 119:142
h Zb 119:33
i Zb 31:8
Zb 118:5
j Zb 119:94
Zb 119:141
k 2Sa 12:7
Zb 93:5
Zb 119:168
Da 5:22
Mt 10:18
Mdo 26:2
l Mk 8:38
Ro 1:16
m Zb 112:1
n Ayu 23:12
Zb 119:174
Ro 7:22
o Zb 119:127
Mhu 12:13
p Zb 119:23
Zb 119:71
q 2Sa 7:25
Zb 105:42
Zb 106:45
r Zb 71:14
s Zb 94:19
Ro 15:4

Safu ya 2

a Zb 119:25
b Zb 123:4
Met 9:12
c Ayu 23:11
Zb 44:18
Zb 119:157
d Hes 16:5
Kum 1:35
Kum 4:3
Zb 36:6
Zb 105:5
e Ro 15:4
f Ezr 9:13
Zb 119:158
Zb 139:21
g Met 28:4
h Zb 119:112
i Mwa 47:9
Ebr 11:13
j Zb 42:8
Zb 63:6
Isa 26:9
k Zb 119:34
l Zb 119:100
m Zb 16:5
Zb 73:26
Yer 10:16
n Kut 19:8
2Fa 23:3
Zb 106:12
o Kut 32:11
2Nya 34:27
Zb 51:17
p Zb 26:11
Zb 57:1

q Zb 119:101; Lu 15:18; 2Ko 13:5; Efe 5:15; r Kum 4:30; Zb 119:146; Yer 31:18; s Kut 7:20; 2Nya 29:3; Mdo 16:33; t Met 7:2.

61 Kamba za waovu
zilinizingira.[a]
Sikuisahau sheria yako.[b]
62 Katikati ya usiku
mimi huamka ili
kukushukuru[c]
Kwa ajili ya maamuzi
yako ya hukumu ya
uadilifu.[d]
63 Mimi ni mwenzao watu
wote wanaokuogopa
wewe,[e]
Na wale wanaoyashika
maagizo yako.[f]
64 Fadhili zako zenye
upendo, Ee Yehova,
zimeijaza dunia.[g]
Unifundishe masharti
yako mwenyewe.[h]

ט [*Tehth*]

65 Umemtendea mtumishi
wako vema,[i]
Ee Yehova, kulingana na
neno lako.[j]
66 Unifundishe wema,[k]
kuwa na akili[l] na
ujuzi,[m]
Kwa maana nimeonyesha
imani katika amri
zako.[n]
67 Kabla ya kuteseka
nilikuwa nikifanya
dhambi bila
kukusudia,[o]
Bali sasa nimelishika
neno lako.[p]
68 Wewe ni mwema nawe
unatenda mema.[q]
Unifundishe masharti
yako.[r]
69 Wenye kimbelembele
wamenipaka uwongo.[s]
Bali mimi, nitayashika
maagizo yako kwa moyo
wangu wote.[t]
70 Moyo wao umekosa hisia
kama mafuta.[u]
Mimi nami,
nimependezwa na
sheria yako.[v]

SURA 119

a Zb 140:5
Yer 38:6
b 1Sa 26:9
2Nya 29:2
c Zb 42:8
Mdo 16:25
d Ne 9:13
e Zb 16:3
Zb 142:7
Met 13:20
Mal 3:16
f Zb 119:56
g Zb 33:5
Zb 104:13
h 1Fa 8:58
Zb 119:33
Zb 119:124
i Mwa 39:3
1Sa 18:14
Zb 30:11
j Zb 119:25
k Tit 1:8
l 1Sa 25:33
Da 2:14
m 1Fa 3:9
2Nya 1:10
Zb 94:10
Da 2:21
Flp 1:9
n Zb 106:12
o Law 5:17
Ga 6:1
1Ti 1:13
p Zb 119:11
Ebr 12:11
q Zb 86:5
Zb 106:1
Zb 107:1
Mk 10:18
r Zb 119:12
Isa 48:17
s Ayu 13:4
Zb 86:14
Zb 109:2
Zb 119:51
t Zb 19:8
Zb 119:40
u Zb 17:10
Isa 6:10
Mdo 28:27
v Zb 40:8
Ro 7:22

Safu ya 2

a 1Ko 11:32
Ebr 5:8
Ebr 12:10
b Kum 4:14
Zb 119:171
c Kum 17:19
d Zb 19:7
e Zb 19:10
Zb 119:127
wake wa kushoto.[i] **3** Pia, katika njia yoyote ambayo mtu
mpumbavu anatembea,[j] moyo
wake mwenyewe una kasoro,
naye hakika humwambia kila
mtu kwamba yeye ni mpumbavu.[k]
4 Roho ya mtawala ikiinuka juu yako, usiondoke mahali pako,[l] kwa maana utulivu
wenyewe hutuliza dhambi kubwa.[m]
5 Kuna jambo lenye msiba ambalo nimeona chini ya
jua, kama wakati ambapo kuna
kosa[n] linalotokea kwa sababu
ya mtu aliye katika mamlaka:[o]
6 Upumbavu umewekwa katika vyeo vingi vya juu,[p] lakini matajiri huendelea kukaa tu
katika hali ya chini.
7 Nimeona watumishi juu
ya farasi lakini wakutembea kwa miguu juu ya nchi
kama watumishi tu.[a]
8 Anayechimba shimo yeye
mwenyewe ataanguka ndani
yake;[b] naye anayebomoa ukuta
wa mawe ataumwa na nyoka.[c]
9 Anayechimba mawe atajiumiza mwenyewe kwayo. Naye
anayepasua miti atalazimika
kujihadhari nayo.[d]
10 Ikiwa kifaa cha chuma
kimepoteza makali na mtu asikinoe,[e] ndipo atatumia nguvu
zake mwenyewe. Kwa hiyo kutumia hekima kwa mafanikio
huleta faida.[f]
11 Nyoka akiuma kabla ya
kuchezeshwa,[g] basi mtu anayejua kuutumia ulimi hapati faida yoyote.
12 Maneno ya kinywa cha
mwenye hekima huleta kibali,[h]
bali mjinga humezwa na midomo yake.[i] **13** Mwanzo wa maneno ya kinywa chake ni upumbavu,[j] na mwisho wa kinywa
chake ni wazimu wenye msiba.
14 Na mpumbavu husema maneno mengi.[k]
Mwanadamu hajui jinsi mambo yatakavyokuwa; na yale
yatakayotokea baada yake, ni
nani anayeweza kumwambia?[l]
15 Kazi ngumu ya wajinga
huwachosha,[m] kwa sababu hakuna hata mmoja amekuja kujua jinsi ya kwenda jijini.[n]
16 Ewe nchi, itakuwaje kwako wakati mfalme wako ni mvulana[o] na wakuu wako huendelea kula hata asubuhi? **17** Ewe
nchi, una furaha wakati mfalme wako ni mwana wa watu
wenye vyeo na wakuu wako
hula wakati unaofaa ili kuwa na

SURA 9
a Met 21:22 Met 24:5 Mhu 7:19 Mhu 9:18
b Met 10:15 (Mr 6:3 Yn 7:48 1Ko 1:27 1Ko 2:8
c Mwa 41:39 Met 22:17 Dan 12:3
d 1 Sa 7:3
e Yos 22:20 1Ko 5:6 Ga 5:9 Tit 1:11 Ebr 12:15 3Yh 10

SURA 10
f Kut 30:35
g He 20:12 2 Sa 12:12
h Met 14:8 Mt 25:33 Lu 14:28
i Met 17:16 Mhu 10:14 Mt 25:41
j Met 10:23 Met 18:6 1Pe 4:4
k Met 13:16 Met 18:7 Met 29:11 Mhu 5:3
l 1 Fal 2:36 Mhu 8:3 Tit 3:2
m 1 Sa 25:24 Met 25:15
n 1 Fal 12:10
o 1 Sa 26:21 Isa 3:12
p 1 Fal 12:14 Est 3:1 Met 28:12 Mhu 4:13

Safu ya 2
a 2 Sa 3:39 Met 19:10 Met 30:22 Isa 3:5
b 2 Sa 17:23 Est 7:10 Zab 7:15 Zab 9:15 Met 26:27
c Amo 5:19 Amo 9:3
d Kum 19:5
e 1 Sa 13:20
f Kut 31:3 2 Nya. 2:14 Mhu 9:10
g Zab 58:5 Yer 8:17
h 1 Fal 10:8 Ayu 4:4 Zab 37:30 Met 10:21 Lu 4:22 Efe 4:29
i Zab 64:8 Met 10:14 Met 14:3
j 1 Sa 20:31 1 Sa 25:10 2 Fal 6:31 Lu 6:11
k Met 10:19 Met 15:2

l Met 27:1; Mhu 6:12; Mhu 8:7; Yak 4:14; m Hab 2:13; n Zab 107:4; o 2 Nya. 13:7; 2 Nya. 36:9; Isa 3:4.

uwezo, wala si kwa ajili ya kunywa tu.[a]

18 Kwa sababu ya uvivu mkubwa paa ya jengo hubonyea, na kwa kushusha mikono, nyumba huvuja.[b]

19 Mkate ni kwa ajili ya kicheko cha wafanyakazi, na divai hufanya maisha yafurahishe;[c] lakini pesa ndizo hutokeza jibu katika mambo yote.[d]

20 Hata katika chumba chako cha kulala usimlaani mfalme,[e] na katika chumba cha ndani unapolala usimlaani yeyote aliye tajiri;[f] kwa maana kiumbe kinachoruka cha mbinguni kitafikisha sauti hiyo na kiumbe chenye mabawa kitasema jambo hilo.[g]

11 Tupa mkate[h] wako juu ya uso wa maji,[i] kwa maana baada ya siku nyingi utaupata tena.[j] **2** Wape fungu watu saba, au hata wanane,[k] kwa maana hujui ni msiba gani utakaotokea duniani.[l]

3 Mawingu yakijaa maji, humwaga mvua kubwa juu ya dunia;[m] nao mti ukianguka kuelekea kusini au kaskazini, mahali hapo hapo ulipoanguka[n] ndipo utakapokuwa.

4 Anayeuangalia upepo hatapanda mbegu; naye anayetazama mawingu hatavuna.[o]

5 Kama vile usivyoijua njia ya roho katika mifupa ndani ya tumbo lake mwenye mimba,[p] vivyo hivyo hujui kazi ya Mungu wa kweli, anayefanya mambo yote.[q]

6 Asubuhi panda mbegu zako na mpaka jioni usiache mkono wako upumzike;[r] kwa maana hujui ni wapi hii itafanikiwa,[s] hapa au pale, au ikiwa zote mbili zitakuwa njema.

SURA 10

a Met 31:4
Isa 28:7
Hos 7:5
b Met 21:25
Met 24:33
Ebr 6:12
c Zab 104:15
Mhu 9:7
d Mhu 7:12
Lu 16:9
e Kut 22:28
Isa 8:21
1Pe 2:13
f Mhu 7:12
g Lu 12:2

SURA 11

h Ne 8:10
Est 9:19
i Kum 15:11
Met 22:9
Isa 32:20
j Kum 15:10
Zab 41:1
Met 19:17
Lu 14:14
Ebr 6:10
k Zab 37:21
Lu 6:38
Mdo 4:32
2Ko 9:7
1Ti 6:18
l Dan 4:27
m 1 Fal 18:45
Isa 55:10
n Ayu 14:7
o Met 20:4
Met 24:34
p Ayu 10:11
Zab 139:13
Zab 139:15
Yer 1:5
q Ayu 11:7
Ayu 26:14
Zab 40:5
Mhu 8:17
Ro 11:33
r Mhu 9:10
Hos 10:12
Yn 9:4
2Ko 9:6
Kol 3:23
s Met 27:1
Yak 4:14

Safu ya 2

a Ayu 33:28
Met 29:13
Mhu 7:11
b Mhu 5:18
Mhu 8:15
c Mwa 48:10
Mhu 12:2
Yn 21:18
d Mhu 2:11
Mhu 4:8
e Kum 16:11
Zab 5:11
f Ayu 31:7
g Mhu 3:17
Mhu 12:14
Ro 2:6
Ro 14:12
2Ko 5:10
h Ayu 13:26
Zab 25:7
i Mhu 12:8
2Ti 2:22

SURA 12

j Mwa 1:1
Mwa 1:27

7 Nuru ni tamu pia, na ni vema macho yaone jua;[a] **8** kwa maana mwanadamu akiishi miaka mingi, na aishangilie hiyo yote.[b] Na azikumbuke siku za giza,[c] ingawa huenda zikawa nyingi; kila siku ambayo imekuja ni ubatili.[d]

9 Ewe kijana, shangilia[e] katika ujana wako, na moyo wako ukufanyie mema siku za ujana wako, nawe utembee katika njia za moyo wako na katika mambo ambayo macho yako yameona.[f] Lakini ujue kwamba kwa ajili ya mambo yote hayo, Mungu wa kweli atakuleta hukumuni.[g] **10** Kwa hiyo, ondoa masumbuko moyoni mwako, nawe uondolee mbali msiba kutoka katika mwili wako;[h] kwa maana ujana na upeo wa maisha ni ubatili.[i]

12 Mkumbuke, sasa, Muumba wako Mkuu katika siku za ujana wako,[j] kabla siku zenye msiba hazijaja,[k] au miaka iwe imefika wakati utasema:! "Sipendezwi nayo";[m] **2** kabla jua na nuru na mwezi na nyota havijawa na giza,[n] na mawingu yamerudi, kisha mvua kubwa; **3** katika siku ambayo watunzaji wa nyumba[o] wanatetemeka, nao wanaume wenye nguvu wameinama,[p] na wanawake wanaosaga[q] wameacha kufanya kazi kwa sababu wamekuwa wachache, na mabibi wanaochungulia madirishani[r] wameona giza; **4** na milango inayoelekea barabarani imefungwa,[s] wakati sauti ya jiwe la kusaga inaposhuka,[t] naye mtu

k Zab 71:17; Zab 110:3; Zab 148:12; Lu 2:49; 2Ti 3:15; l Zab 90:10; m 2 Sa 19:35; n Mwa 27:1; 1 Sa 4:15; o Ayu 4:19; Mt 12:44; 2Ko 5:1; 2Pe 1:13; p 2 Sa 21:15; Zab 22:15; Zab 90:9; Zab 102:23; q Ayu 31:10; Isa 47:2; Mt 24:41; r Mwa 48:10; Isa 59:10; Mt 9:29; s Ayu 41:14; t Zab 58:6.

huamshwa na sauti ya ndege, na
mabinti wote wa wimbo hutoa sa-
uti ya chini.[a] **5** Pia, wameogo-
pa chochote kilicho juu, na kuna
vitisho njiani. Nao mti unao-
zaa lozi hutoa maua,[b] naye pa-
nzi hujikokota, na pilipili hu-
pasuka, kwa sababu mwanada-
mu anakwenda kwenye nyumba
yake ya muda mrefu,[c] nao wao-
mbolezaji wamezunguka barabara-
ni;[d] **6** kabla ile kamba ya fe-
dha haijaondolewa, na bakuli
la dhahabu kuvunjwa,[e] na
mtungi ulio kwenye bubujiko la
maji kuvunjwa, na gurudumu
la maji kuvunjwa. **7** Kisha ma-
vumbi huirudia nchi[f] kama ya-
livyokuwa, nayo roho[g] yenyewe
humrudia Mungu[h] wa kweli ali-
yeitoa.[i]

8 "Ubatili mkubwa zaidi!"
akasema mkutanishaji,[j] "Kila
kitu ni ubatili."[k]

9 Na ijapokuwa mkutani-
shaji alipata kuwa na hekima,[l]
pia aliendelea kuwafundisha
watu ujuzi,[m] naye alitafakari
na kutafuta kwa bidii,[n] apa-
te kupanga methali nyingi kwa
utaratibu.[o] **10** Mkutanishaji

SURA 12

a 2Sa 19:35
b Ayu 15:10
Met 16:31
c Ayu 17:13
Ayu 30:23
Zab 49:14
Mhu 9:10
d Mwa 50:10
(Mr 5:38
e Amu 9:53
f Mwa 3:19
Ayu 34:15
Zab 146:4
Mhu 3:20
g Ayu 34:14
Zab 104:29
Mhu 3:21
h 1Ko 8:4
i Mwa 2:7
Ayu 27:3
Isa 42:5
Zek 12:1
j 1Fal 8:1
k Mhu 1:2
Mhu 1:14
l 1Fal 3:12
1Fal 10:23
m 1Fal 10:3
1Fal 10:8
n Met 25:2
Lu 1:3
o 1Fal 4:32
Met 1:1

Safu ya 2

a Met 15:23
Met 16:21
Met 16:24
Met 25:11
b Lu 1:4
Yn 17:17
c Mdo 2:37
2Ko 10:4
Tit 2:4
Ebr 4:12
d Zab 112:8
1Ko 15:58
Efe 6:14

alijitahidi kutafuta maneno
yenye kupendeza[a] na kuandika
maneno sahihi ya kweli.[b]

11 Maneno ya wenye heki-
ma ni kama michokoo ya ku-
ongoza ng'ombe,[c] na kama tu
misumari iliyopigiliwa nda-
ni,[d] ndivyo walivyo wale wa-
naoshughulika mno kukusa-
nya maneno; wametolewa ku-
toka kwa mchungaji mmoja.[e]
12 Kuhusu jambo lingine lolote
zaidi ya haya, mwanangu,
jihadhari: Hakuna mwisho wa
kutungwa kwa vitabu vingi, na
kushughulika navyo sana huu-
chosha mwili.[f]

13 Huu ndio mwisho wa ma-
mbo, kila jambo limekwisha si-
kiwa: Mwogope Mungu wa kwe-
li[g] na kushika amri zake.[h] Kwa
maana huo ndio wajibu wote wa
mwanadamu. **14** Kwa maana
Mungu wa kweli ataleta kila kazi
katika hukumu, kuhusiana na
kila jambo lililofichwa, liwe jema
au baya.[i]

e Zab 23:1; Zab 80:1; 1Pe 5:4; f Mhu 1:18; Mdo 19:19; Kol 2:8; g Kum 10:12; Ayu 28:28; Zab 111:10; Met 1:7; Met 8:13; Met 9:10; h Kum 6:2; Zab 119:35; 1Pe 2:17; 1Yh 5:3; i Zab 62:12; Mhu 11:9; Mt 12:36; Lu 12:2; Mdo 17:31; 1Ko 4:5; 2Ko 5:10; 1Ti 5:24.

WIMBO WA SULEMANI

1 Wimbo ulio bora,[a] ambao ni
wa Sulemani:[b] **2** "Na ani-
busu kwa busu za kinywa cha-
ke,[c] maana maonyesho yako
ya mapenzi ni bora kuliko di-
vai.[d] **3** Maana harufu ya ma-
futa yako[e] ni nzuri. Kama ma-
futa yanayomiminwa, ndivyo
lilivyo jina lako.[f] Hiyo ndiyo sa-
babu wanawali wamekupenda.
4 Nivute nyuma yako;[g] na tu-

SURA 1

a Kut 15:1
Kum 31:19
Amu 5:1
2Sa 22:1
Zb 18:Uta
Isa 5:1
Ufu 15:3
b 1Fa 4:32
c Wim 8:1
d Wim 4:10
e Met 27:9
Mhu 9:8
Wim 5:5
Lu 23:56
f Mhu 7:1
g Yoh 6:44

kimbie. Mfalme ameniingiza
katika vyumba vyake vya nda-
ni![a] Na tufurahi na kushangi-
lia katika wewe. Na tutaje ma-
onyesho yako ya mapenzi ku-
liko divai.[b] Wamekupenda ina-
vyostahili.[c]

5 "Mimi ni msichana mweusi,
lakini mwenye kupendeza, enyi

Safu ya 2 a 1Fa 7:1; b Yoh 15:13; c Mt 10:37.

binti za Yerusalemu,[a] kama mahema ya Kedari,[b] tena kama vitambaa vya mahema[c] ya Sulemani. **6** Msinitazame kwa sababu mimi ni mweusi, kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mama yangu mwenyewe walinikasirikia; waliniweka kuwa mtunzaji wa mashamba ya mizabibu,[d] ijapokuwa sikulitunza shamba langu mwenyewe la mizabibu.

7 "Niambie, ewe ambaye nafsi yangu imekupenda,[e] mahali unapochunga,[f] mahali unapolaza kundi katikati ya mchana. Kwa nini niwe kama mwanamke aliyefungwa nguo za maombolezo kati ya makundi ya wenzako?"

8 "Ikiwa wewe mwenyewe hujui, ewe uliye mrembo zaidi kati ya wanawake,[g] nenda mwenyewe katika nyayo za kundi uchunge wana-mbuzi wako kando ya maskani za wachungaji."

9 "Nimekufananisha na farasi-jike wangu katika magari ya Farao,[h] ewe msichana mwenzi wangu.[i] **10** Mashavu yako yanapendeza kati ya nywele zilizosukwa, shingo yako katika mkufu wa shanga.[j] **11** Tutakufanyia vitaji vya dhahabu,[k] pamoja na vifungo vya fedha."

12 "Maadamu mfalme yupo penye meza yake ya mviringo, marashi[l] yangu mwenyewe ya nardo yametoa harufu[m] yake nzuri. **13** Kwangu mimi mpenzi wangu ni kama mfuko wa manemane;[n] katikati ya maziwa[o] yangu atalala usiku kucha. **14** Kama kishada cha hina[p] ndivyo alivyo mpenzi wangu kwangu, kati ya mashamba ya mizabibu ya En-gedi."[q]

SURA 1

a Zb 45:9
b Zb 120:5
Eze 27:21
c Kut 36:14
d Wim 8:12
e 1Sa 18:20
Isa 5:1
f Wim 6:3
Yoh 10:11
Ufu 7:17
g Zb 45:9
Efe 5:27
h 1Fa 10:28
i Wim 6:4
j Eze 16:11
k 2Sa 1:24
Yer 4:30
l Wim 4:13
m Yoh 12:3
n Kut 30:23
Est 2:12
Zb 45:8
Wim 4:6
Wim 5:13
Yoh 19:39
o Wim 4:5
p Wim 4:13
q Yos 15:62

Safu ya 2

a Zb 45:11
Wim 4:7
b Mwa 29:17
Wim 4:1
Wim 5:2
c Zb 45:2
Wim 5:10
Yoh 1:14
Ebr 11:23
d Ayu 7:13
Zb 132:3
e Zb 92:12
Isa 9:10

SURA 2

f Isa 35:1
g 1Nya 27:29
h Wim 2:16
i Wim 1:15
Flp 2:15
1Pe 2:12
j Wim 8:5
k Zb 45:2
Wim 5:9
l Isa 25:6
m Wim 6:4
n Mwa 29:18
Mwa 29:20
o 1Sa 30:12
2Sa 6:19
p 1Sa 18:20
Wim 5:8
q Wim 8:3
r Kum 6:13
s 2Sa 2:18
1Nya 12:8
Wim 3:5
t Met 5:19
u Wim 8:4
v Wim 5:2
Yoh 10:27
Ufu 3:20
w Ufu 22:20
x Wim 2:17
Wim 8:14

15 "Tazama! Wewe ni mrembo, ewe msichana mwenzi wangu.[a] Tazama! Wewe ni mrembo. Macho yako ni kama ya njiwa."[b]

16 "Tazama! Wewe ni mrembo,[c] mpenzi wangu, pia mwenye kupendeza. Pia kitanda[d] chetu ni cha majani. **17** Nguzo za nyumba yetu kuu ni mierezi,[e] maboriti yetu ni miberoshi.

2 "Mimi ni zafarani[f] tu ya nchi tambarare ya pwani,[g] yungiyungi la nchi tambarare za chini."[h]

2 "Kama yungiyungi katikati ya magugu yenye miiba, ndivyo alivyo msichana mwenzi wangu katikati ya mabinti."[i]

3 "Kama mtofaa[j] katikati ya miti ya msituni, ndivyo alivyo mpenzi wangu katikati ya wana.[k] Kivuli chake nimekitamani sana, na hapo nimekaa chini, na matunda yake yamekuwa matamu kinywani mwangu. **4** Alinileta ndani ya nyumba ya divai,[l] na bendera[m] yake juu yangu ilikuwa upendo.[n] **5** Enyi watu niburudisheni kwa keki za zabibu,[o] nitegemezeni kwa matofaa; kwa maana mimi nimelewa mapenzi.[p] **6** Mkono wake wa kushoto uko chini ya kichwa changu; nao mkono wake wa kuume unanikumbatia.[q] **7** Nimewaapisha ninyi,[r] enyi binti za Yerusalemu, kwa swala-jike[s] au kwa paa[t] wa porini, kwamba msijaribu kuamsha au kuwasha upendo ndani yangu mpaka wenyewe utake.[u]

8 "Sauti ya mpenzi wangu![v] Tazama! Anakuja,[w] akipanda juu milimani, akiruka juu vilimani. **9** Mpenzi wangu anafanana na swala[x] au mtoto wa

paa. Tazama! Anasimama nyuma ya ukuta wetu, akichungulia madirishani, akitazama kupitia pazia.[a] **10** Mpenzi wangu amejibu na kuniambia, 'Simama, ewe msichana mwenzi wangu, mrembo wangu,[b] twende zetu.[c] **11** Kwa maana, tazama! msimu wa mvua[d] umepita, mvua kubwa imekwisha, imekwenda zake. **12** Maua yametokea katika nchi,[e] wakati wa kukata matawi ya mizabibu[f] umefika, na sauti ya njiwa-tetere[g] imesikiwa katika nchi yetu. **13** Mtini[h] nao umepevusha rangi ya tini zake za mapema;[i] nayo mizabibu imechanua, imetoa harufu yake nzuri. Simama, njoo, ewe msichana mwenzi wangu,[j] mrembo wangu, twende zetu. **14** Ewe njiwa wangu[k] katika makimbilio ya mwamba, katika mahali palipofichika pa njia yenye mwinuko mkali, nionyeshe umbo lako,[l] acha nisikie sauti yako, kwa maana sauti yako ni tamu na umbo lako ni lenye kupendeza.'"[m]

15 "Tukamatieni mbweha,[n] wale mbweha wadogo wanaoharibu mashamba ya mizabibu, kwa maana mashamba yetu ya mizabibu yamechanua."[o]

16 "Mpenzi wangu ni wangu nami ni wake.[p] Anachunga[q] katikati ya mayungiyungi.[r] **17** Mpaka mchana uvumishe upepo mtulivu na vivuli viwe vimekimbia, geuka, ewe mpenzi wangu; uwe kama swala[s] au kama watoto wa paa juu ya milima ya kutenganisha.

3 "Nyakati za usiku kitandani mwangu nimemtafuta yeye ambaye nafsi yangu imempenda.[t] Nilimtafuta, nisimpate. **2** Tafadhali niache niamke, niende kuzunguka jijini;[a] barabarani na katika viwanja vya watu wote,[b] niache nimtafute yeye ambaye nafsi yangu imempenda. Nilimtafuta, nisimpate. **3** Walinzi[c] waliokuwa wakizunguka jijini walinikuta, 'Je, mmemwona yeye ambaye nafsi yangu imempenda?' **4** Punde tu baada ya kuwaacha nikampata yeye ambaye nafsi yangu imempenda. Nikamkamata, nisimwachilie, mpaka nilipokuwa nimemleta katika nyumba ya mama yangu na katika chumba cha ndani cha yeye aliyekuwa amenichukua mimba. **5** Nimewaapisha[d] ninyi, enyi binti za Yerusalemu, kwa swala-jike au kwa paa wa porini,[e] kwamba msijaribu kuamsha au kuwasha upendo ndani yangu mpaka wenyewe utake."[f]

6 "Ni nini hiki kinachokuja kutoka nyikani kama nguzo za moshi, kikiwa kimetiwa harufu ya manemane na ubani,[g] pamoja na kila namna ya poda ya marashi ya mfanya-biashara?"[h]

7 "Tazama! Ni kitanda chake, kile cha Sulemani. Wanaume 60 wenye nguvu wamekizunguka, kutoka kati ya wanaume wenye nguvu wa Israeli,[i] **8** wote wana upanga, wamefundishwa vita, kila mmoja na upanga wake pajani mwake kwa sababu ya hofu wakati wa usiku."[j]

9 "Ni kitanda ambacho Mfalme Sulemani amejifanyizia kwa miti ya Lebanoni.[k] **10** Nguzo zake amezifanya kwa fedha, vitegemezo vyake kwa dhahabu. Kiti chake ni cha sufu iliyotiwa rangi ya zambarau, ndani yake binti za Yerusale-

SURA 2
a Amu 5:28
b Wim 4:7
c Zb 45:10
Yoh 14:3
d Zek 10:1
e Wim 6:11
Isa 55:10
f Isa 18:5
Yoh 15:2
g Yer 8:7
h Mik 4:4
i Isa 28:4
Nah 3:12
j Wim 1:15
k Wim 5:2
Yer 48:28
Mt 10:16
l Zb 45:11
m Wim 1:5
Wim 6:10
n Amu 15:4
Omb 5:18
o Wim 7:12
p Wim 6:3
Wim 7:10
q Wim 1:7
r Wim 2:1
s 2Sa 2:18
Wim 2:9
Wim 8:14

SURA 3
t 1Sa 18:20
Wim 1:7

Safu ya 2
a 2Nya 9:30
b Ne 8:16
Omb 4:18
c Zb 130:6
Wim 5:7
d 1Fa 22:16
e Wim 2:7
f Wim 8:4
g Yer 2:2
h Kut 30:23
Kut 30:34
i 1Fa 9:22
j Ne 4:22
Mhu 5:12
k 1Fa 5:9

mu wamekipamba vifaa kwa
upendo."
11 "Enyi binti za Sayuni, ne-
ndeni nje mtazame Mfalme Su-
lemani akiwa na shada[a] amba-
lo mama yake[b] alimfumia siku
ya arusi yake na siku ya moyo
wake kushangilia."[c]

4 "Tazama! Wewe ni mre-
mbo,[d] ewe msichana mwe-
nzi wangu. Tazama! Wewe ni
mrembo. Macho yako ni kama
ya njiwa,[e] nyuma ya ushungi
wako.[f] Nywele zako ni kama
kundi la mbuzi[g] ambao wame-
ruka chini kutoka eneo lenye
milima la Gileadi.[h] **2** Meno
yako ni kama kundi la kondoo-
jike waliokatwa manyoya hivi
karibuni[i] ambao wamepanda
kutoka kuoshwa, wote wana-
zaa mapacha, wala hakuna ye-
yote kati yao amepoteza wa-
toto wake. **3** Midomo yako
ni kama tu uzi mwekundu, na
maneno yako yanakubalika.[j]
Kama kipande cha komama-
nga ndivyo yalivyo mashavu
yako nyuma ya ushungi wako.[k]
4 Shingo yako[l] ni kama mna-
ra[m] wa Daudi, uliojengwa kwa
mistari ya mawe, ambao juu
yake hutungikwa ngao elfu,
ngao zote za mviringo[n] za wa-
naume wenye nguvu. **5** Mazi-
wa yako mawili[o] ni kama wato-
to wadogo wawili, mapacha ya
swala-jike, ambao wanalisha
katikati ya mayungiyungi."[p]
6 "Mpaka mchana uvume
upepo mtulivu[q] na vivuli viwe
vimekimbia, nitakwenda za-
ngu kwenye mlima wa mane-
mane na kwenye kilima cha
ubani."[r]
7 "Wewe ni mrembo kabi-
sa,[s] ewe msichana mwenzi wa-
ngu, wala hamna kasoro ndani
yako.[a] **8** Na uje pamoja nami
kutoka Lebanoni, ewe bibi-aru-
si,[b] uje pamoja nami kutoka
Lebanoni.[c] Ushuke kutoka ki-
lele cha Milima ya Anti-Leba-
noni, kutoka kilele cha Se-
niri,[d] naam, Hermoni,[e] kuto-
ka katika matundu ya simba,
kutoka katika milima ya chui.
9 Umefanya moyo wangu upi-
ge, ewe dada yangu,[f] bibi-aru-
si wangu,[g] umefanya moyo wa-
ngu upige kwa moja la macho
yako,[h] kwa kidani kimoja cha
mkufu wako. **10** Jinsi yali-
vyo mazuri maonyesho yako ya
mapenzi,[i] ewe dada yangu, bibi-
arusi wangu! Jinsi maonyesho
yako ya mapenzi yalivyo bora
kuliko divai na harufu nzuri
ya mafuta yako kuliko namna
zote za manukato![j] **11** Mido-
mo yako inadondosha asali ya
sega,[k] ewe bibi-arusi wangu.
Asali[l] na maziwa viko chini ya
ulimi wako, na harufu nzuri ya
mavazi yako ni kama harufu
nzuri[m] ya Lebanoni. **12** Dada
yangu,[n] bibi-arusi wangu, ni bu-
stani iliyowekewa boma, bubu-
jiko lililofungwa kwa kutiwa
muhuri. **13** Ngozi yako ni pa-
radiso ya makomamanga, ye-
nye matunda bora kabisa,[o] mi-
mea ya hina pamoja na mimea
ya nardo;[p] **14** nardo[q] na zafa-
rani,[r] kane[s] na mdalasini,[t] pa-
moja na namna zote za miti
ya ubani, manemane na udi,[u]
pamoja na manukato yote ya-
liyo bora zaidi;[v] **15** na bubuji-
ko la bustani, kisima cha maji
safi,[w] na vijito vinavyotiririka
kutoka Lebanoni.[x] **16** Amka,
ewe upepo wa kaskazini, ingia,
ewe upepo wa kusini.[y] Vuma
juu ya bustani yangu.[z] Manuka-
to yake na yatiririke."

SURA 3
a Met 4:9
b 2Sa 12:24
Met 4:3
c Isa 62:5

SURA 4
d Zb 45:11
e Wim 1:15
f Mwa 24:65
g Wim 6:5
h Hes 32:1
Kum 3:12
i Wim 6:6
j Zb 37:30
Zb 45:2
k Wim 6:7
l Wim 1:10
m Ne 3:25
Wim 7:4
n 2Sa 8:7
2Fa 11:10
Eze 27:11
o Wim 7:3
p Wim 2:16
q Wim 2:17
r Mhu 2:5
s Wim 4:1

Safu ya 2
a 2Ko 11:2
Efe 1:4
2Pe 3:14
b Yoh 3:29
Ufu 21:9
c Kum 3:25
d Kum 3:9
e Zb 133:3
f Wim 5:1
g Zb 45:14
Ufu 19:7
h Met 5:19
i Wim 1:2
Wim 7:12
j Est 2:12
Wim 1:3
Wim 1:12
k Met 16:24
l Met 24:13
Wim 5:1
m Zb 45:8
n Wim 6:2
o Wim 7:13
p Wim 1:12
q Yoh 12:3
r Wim 2:1
s Kut 30:23
Isa 43:24
t Met 7:17
Ufu 18:13
u Hes 24:6
Zb 45:8
v Kut 30:34
Eze 27:22
2Ko 2:14
w Mwa 26:19
x Yer 18:14
y Mhu 1:6
z Wim 5:1

"Mpenzi wangu na aje katika bustani yake, ale matunda yake yaliyo bora kabisa."

5 "Nimeingia katika bustani yangu,[a] ewe dada yangu,[b] bibi-arusi wangu.[c] Nimechuma manemane[d] yangu pamoja na manukato yangu. Nimekula sega langu la asali pamoja na asali yangu;[e] nimekunywa divai yangu pamoja na maziwa yangu."

"Kuleni, enyi wapenzi! Kunyweni, mlewe maonyesho ya mapenzi!"[f]

2 "Mimi nimelala, bali moyo wangu umeamka.[g] Kuna sauti ya mpenzi wangu akipiga hodi!"[h]

"Nifungulie,[i] ewe dada yangu, msichana mwenzi wangu, njiwa wangu, wangu asiye na lawama![j] Maana kichwa changu kimejaa umande, mashungi ya nywele zangu yamejaa matone ya usiku."[k]

3 "'Nimevua kanzu yangu. Naweza kuivaaje tena? Nimeosha miguu yangu. Naweza kuichafuaje?' **4** Mpenzi wangu alirudisha nyuma mkono wake kutoka kwenye tundu la mlango, na tumbo[l] langu likawa na msukosuko ndani yangu. **5** Mimi mwenyewe nikasimama nimfungulie mpenzi wangu. Mikono yangu ikadondoka manemane na vidole vyangu manemane ya majimaji, juu ya matundu ya kufuli. **6** Mimi mwenyewe nikamfungulia mpenzi wangu, kumbe mpenzi wangu alikuwa amegeuka, alikuwa amepita. Nafsi yangu ilikuwa imenitoka alipoongea. Nikamtafuta, nisimpate.[m] Nikamwita, asiniitikie. **7** Walinzi[n] waliokuwa wakizunguka jijini wakanikuta. Wakanipiga, wakaniumiza. Walinzi wa kuta[a] wakanivua kifuniko changu kipana.

8 "Nimewaapisha[b] ninyi, enyi binti za Yerusalemu,[c] kwamba, mkimpata mpenzi wangu,[d] mwambieni kuwa mimi nimelewa mapenzi."[e]

9 "Jinsi gani mpenzi wako ni bora kuliko mpenzi mwingine yeyote,[f] ewe uliye mrembo zaidi kati ya wanawake?[g] Jinsi gani mpenzi wako ni bora kuliko mpenzi mwingine yeyote, hata ukatuapisha kwa kiapo cha namna hii?"[h]

10 "Mpenzi wangu anametameta na ni mwekundu, mwenye kuvutia zaidi kati ya elfu kumi.[i] **11** Kichwa chake ni dhahabu, dhahabu safi. Mashungi ya nywele zake ni vishada vya tende. Nywele zake nyeusi ni kama kunguru. **12** Macho yake ni kama njiwa kando ya mifereji ya maji, ambao wanaoga katika maziwa, wakiwa wameketi ndani ya vyombo vya mviringo. **13** Mashavu yake ni kama eneo dogo la bustani ya manukato,[j] minara ya mimea yenye harufu tamu. Midomo yake ni mayungiyungi, inadondosha manemane ya majimaji.[k] **14** Mikono yake ni mianzi ya dhahabu, imejazwa krisolito. Tumbo lake ni bamba la pembe ya tembo lililopambwa kwa yakuti. **15** Miguu yake ni nguzo za marumaru zinazokalia vikalio vya dhahabu safi. Sura yake ni kama Lebanoni, bora kama mierezi.[l] **16** Kinywa chake ni utamu mtupu, na kila kitu kumhusu ni chenye kupendeza kabisa.[m] Huyo ndiye mpenzi wangu, na

SURA 5
a Wim 4:16
Wim 6:2
b Wim 4:9
1Ti 5:2
c Wim 4:8
Yoh 3:29
Ufu 21:9
d Wim 4:14
e Kum 26:9
Wim 4:11
Isa 7:15
f Wim 1:2
Wim 1:4
g Wim 3:1
h Ufu 3:20
i Lu 12:36
j 2Ko 7:1
2Ko 11:2
Efe 5:27
2Pe 3:14
Ufu 14:4
k Lu 2:8
l Mwa 43:30
1Fa 3:26
m Wim 3:1
n Wim 3:3

Safu ya 2
a Isa 62:6
b Kum 6:13
Kum 10:20
c Wim 3:10
d Zb 45:2
e Wim 2:5
f Zb 45:7
g Wim 6:1
h Wim 5:8
i Lu 2:52
j Wim 6:2
k Wim 1:13
l Zb 92:12
m Zb 45:2
Wim 2:3

huyo ndiye mvulana mwenzi
wangu, enyi binti za Yerusale-
mu."

6 "Mpenzi wako amekwenda
wapi, ewe mwanamke mre-
mbo zaidi kati ya wanawake?[a]
Mpenzi wako amegeukia upa-
nde gani, ili tumtafute pamoja
nawe?"

2 "Mpenzi wangu ameshuka
kwenda katika bustani yake,[b]
katika eneo dogo la bustani ya
manukato,[c] kuchunga[d] katikati
ya bustani, na kuchuma mayu-
ngiyungi. **3** Mimi ni wa mpe-
nzi wangu, naye mpenzi wangu
ni wangu.[e] Anachunga[f] katika-
ti ya mayungiyungi."

4 "Wewe ni mrembo, ewe
msichana mwenzi wangu,[g]
kama Jiji la Kupendeza,[h] una-
vutia kama Yerusalemu,[i] una-
tisha kama vikosi[j] vilivyo-
kusanyika kuzunguka be-
ndera.[k] **5** Geuzia mbali ma-
cho yako[l] kutoka mbele yangu,
kwa kuwa yamenishtua mimi.
Nywele zako ni kama kundi
la mbuzi ambao wameruka chi-
ni kutoka Gileadi.[m] **6** Meno
yako ni kama kundi la kondoo-
jike ambao wamepanda kuto-
ka kuoshwa, wote wanazaa ma-
pacha, na kati yao hakuna ye-
yote aliyepoteza watoto wake.[n]
7 Kama kipande cha koma-
manga ndivyo yalivyo masha-
vu yako nyuma ya ushungi
wako.[o] **8** Huenda kuna ma-
lkia 60 na masuria 80 na wana-
wali wasio na hesabu.[p] **9** La-
kini kuna mmoja ambaye ni nji-
wa wangu,[q] wangu asiye na la-
wama.[r] Kuna mmoja ambaye ni
wa mama yake. Yeye ndiye ali-
ye safi wa yule aliyemzaa. Binti
wamemwona, nao wakamta-
ngaza kuwa mwenye furaha;

SURA 6
a Zb 45:11
Wim 1:8
Wim 5:9
Ufu 19:8
b Wim 5:1
c Wim 5:13
d Wim 1:7
Wim 2:16
e Wim 7:10
2Ko 11:2
f Isa 40:11
Yoh 10:14
Ebr 13:20
g Wim 1:9
h 1Fa 14:17
i Zb 48:2
Ufu 21:10
j Wim 6:10
k Zb 20:5
l Wim 1:15
Wim 4:9
Wim 7:4
m Wim 4:1
n Wim 4:2
o Wim 4:3
p 1Fa 11:1
q Wim 2:14
r Wim 5:2

Safu ya 2
a Zb 45:9
Isa 49:23
b Wim 8:5
Ufu 21:10
c 2Sa 23:4
Isa 58:8
d Isa 24:23
e Mt 13:43
f Wim 6:4
g Mhu 2:5
Wim 6:2
h Kum 8:7
i Wim 7:12
j Wim 1:10
k Wim 1:6
Ufu 19:7

SURA 7
l Isa 52:7
Ro 10:15
m Zb 110:3
n Zb 45:13
o Met 9:2
Wim 8:2
p Wim 2:2
q Wim 4:5
r Wim 1:10
Wim 4:4
s Wim 4:1
t Hes 21:25
Yos 21:39
u Isa 35:2
v Wim 6:5

malkia na masuria, nao wakaa-
nza kumsifu,[a] **10** 'Mwana-
mke[b] huyu ni nani, anayeta-
zama chini kama mapambazu-
ko,[c] mrembo kama mwezi mpe-
vu,[d] mwenye kutakata kama
jua linaloangaza,[e] mwenye ku-
tisha kama vikosi vilivyokusa-
nyika kuzunguka bendera?'"[f]

11 "Nilikuwa nimeshuka
kwenda katika bustani[g] ya mi-
lozi, nione matumba katika bo-
nde la mto,[h] nione kama mzabi-
bu ulikuwa umechipuka, kama
mikomamanga ilikuwa imecha-
nua.[i] **12** Kabla sijajua, nafsi
yangu mimi ilikuwa imenitia
katika magari ya watu wangu
wenye kujitoa kwa kupenda."

13 "Rudi, rudi, ewe Mshula-
mi! Rudi, rudi, ili tukutazame!"[j]

"Mnaona nini kwa Mshula-
mi?"[k]

"Kitu kama dansi ya kambi
mbili!"

7 "Jinsi hatua zako zimeku-
wa nzuri katika viatu vya-
ko,[l] ewe binti mwenye kuji-
toa kwa kupenda![m] Mikato ya
mapaja yako ni kama mapa-
mbo,[n] kazi ya mikono ya fu-
ndi. **2** Kitovu chako ni ba-
kuli la mviringo. Divai iliyo-
changanywa[o] isikosekane nda-
ni yake. Tumbo lako ni rundo
la ngano, lililozungushiwa ua
wa mayungiyungi.[p] **3** Mazi-
wa yako mawili ni kama wato-
to wawili, mapacha ya swala-
jike.[q] **4** Shingo yako[r] ni kama
mnara wa pembe ya tembo. Ma-
cho yako[s] ni kama vidimbwi ka-
tika Heshboni,[t] kando ya lango
la Bath-rabimu. Pua yako ni
kama mnara wa Lebanoni,
ambao unaelekea Damasko.
5 Kichwa chako juu yako ni
kama Karmeli,[u] na mashungi[v]

ya nywele za kichwa chako ni
kama sufu iliyotiwa rangi ya
zambarau.[a] Mfalme amenaswa
na mining'inio ya nywele zako.[b]
6 Jinsi ulivyo mrembo, na ji-
nsi unavyopendeza, ewe msi-
chana mpendwa, katikati ya fu-
raha tele![c] **7** Hiki kimo cha-
ko kinafanana na mtende,[d] na
maziwa yako[e] kama vishada
vya tende. **8** Nimesema, 'Ni-
tapanda juu ya mtende, nika-
mate vitawi vya matunda yake
ya tende.'[f] Tafadhali, maziwa
yako na yawe kama vishada
vya mzabibu, na harufu nzu-
ri ya pua yako kama matofaa,
9 na kinywa chako kama di-
vai bora[g] zaidi ambayo inashu-
ka kwa ulaini[h] kwa ajili ya mpe-
nzi wangu, ikitiririka taratibu
juu ya midomo ya wenye kula-
la usingizi."

10 "Mimi ni wa mpenzi wa-
ngu,[i] na tamaa yake imenielek-
ea mimi.[j] **11** Njoo, ewe mpe-
nzi wangu, twende shambani;[k]
tukae katikati ya mimea ya
hina.[l] **12** Na tuamke mape-
ma, twende katika mashamba
ya mizabibu, tuone kama mza-
bibu umechipuka,[m] kama ua li-
mechanuka,[n] kama mikoma-
manga imechanua.[o] Huko nita-
kupa wewe maonyesho yangu
ya mapenzi.[p] **13** Dudai[q] zime-
toa harufu yake nzuri, na ka-
ndo ya maingilio yetu kuna
namna zote za matunda bora
kabisa.[r] Mapya na ya zamani vi-
levile, ewe mpenzi wangu, ni-
mekuwekea hazina.

8 "Laiti ungekuwa kama ndu-
gu yangu,[s] ukinyonya mazi-
wa ya mama yangu![t] Ninge-
kukuta nje, ningekubusu.[u]
Watu hawangenidharau mimi.
2 Ningekuongoza, ningekuleta
ndani ya nyumba ya mama ya-
ngu,[a] aliyekuwa akinifundisha.
Ningekupa kinywaji cha di-
vai iliyotiwa vikolezo,[b] maji safi
ya makomamanga. **3** Mkono
wake wa kushoto ungekuwa
chini ya kichwa changu; nao
mkono wake wa kuume ungeni-
kumbatia.[c]

4 "Nimewaapisha ninyi, enyi
binti za Yerusalemu kwamba
msijaribu kuamsha au kuwa-
sha upendo ndani yangu mpa-
ka wenyewe utake."[d]

5 "Mwanamke[e] huyu ni
nani, anayepanda kutoka nyi-
kani,[f] akimwegemea mpenzi
wake?"[g]

"Chini ya mtofaa nilikuam-
sha. Hapo mama yako aliku-
wa na uchungu wa kukuzaa.
Hapo yeye aliyekuwa akikuzaa
alipata uchungu.[h]

6 "Nitie kama muhuri juu ya
moyo wako,[i] kama muhuri juu
ya mkono wako; kwa maana
upendo una nguvu kama kifo,[j]
msisitizo juu ya kujitoa kika-
mili[k] ni wenye kudai kama Ka-
buri.* Miwako yake ni miwa-
ko ya moto, mwali wa moto
wa Yah.[l] **7** Maji mengi haya-
wezi kuuzima upendo,[m] wala
mito haiwezi kuufagilia mbali.[n]
Kama mtu angetoa vitu vyote
vyenye thamani vya nyumba
yake kwa ajili ya upendo, haki-
ka watu wangevidharau."

8 "Tunaye dada mdogo[o] amba-
ye hana maziwa yoyote. Tuta-
mfanyia nini dada yetu siku
atakapochumbiwa?"

9 "Kama akiwa ukuta,[p] tuta-
jenga juu yake mnara wa fedha;
lakini akiwa mlango,[q] tutamzuia
kwa ubao wa mwerezi."

Wim 8:6* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

SURA 7

a Est 8:15
Wim 3:10
b Wim 1:4
c Wim 4:7
d Zb 92:12
e Wim 7:3
Wim 8:10
f Mt 5:28
1Ti 5:2
g Zb 104:15
h Met 23:31
i Wim 2:16
Wim 6:3
j Wim 2:14
k Wim 8:1
l Wim 1:14
Wim 4:13
m Wim 6:11
n Wim 2:13
o Kum 8:8
Wim 6:11
p Wim 1:4
Wim 4:10
q Mwa 30:14
r Wim 4:16

SURA 8

s Wim 1:6
t Ga 4:26
u Zb 2:12
Wim 1:2

Safu ya 2

a Wim 3:4
b Met 9:2
Wim 5:1
c Wim 2:6
d Wim 2:7
Wim 3:5
e Wim 6:13
Wim 7:10
f Zb 45:10
g Wim 7:11
h Mwa 3:16
i Hag 2:23
j Yoh 15:13
Ro 16:4
Efe 5:25
Ufu 12:11
k Kut 20:5
Yos 24:19
l Zb 89:8
Zb 118:17
Isa 12:2
1Yo 4:8
m 1Ko 13:8
1Ko 13:13
n Ro 8:39
o Wim 1:6
p 2Ko 7:1
Ga 5:23
1Pe 3:2
q Met 7:11
Ho 2:7
1Ko 7:9

10 "Mimi ni ukuta, na maziwa yangu ni kama minara.[a] Basi nimekuwa machoni pake yeye kama msichana anayepata amani.

11 "Kulikuwa na shamba la mizabibu[b] ambalo Sulemani alikuwa nalo katika Baal-hamoni. Aliwapa watunzaji[c] hilo shamba la mizabibu. Kila mmoja alikuwa akileta vipande elfu moja vya fedha kwa ajili ya matunda yake.

SURA 8

a 1Ko 7:34
Kol 3:5
1Pe 2:12
b Mhu 2:4
Wim 7:12
c Lu 20:9

Safu ya 2

a Wim 1:6
Wim 6:11
b Wim 2:14
c Wim 2:17

12 "Shamba langu mwenyewe la mizabibu liko chini ya mamlaka yangu. Nawe, Ee Sulemani una elfu na wale wanaotunza matunda yake wana mia mbili."

13 "Enyi mnaokaa katika bustani,[a] hao wenzi wanasikiliza kwa makini sauti zenu. Acheni niisikie."[b]

14 "Kimbia, mpenzi wangu, ujifanye kama swala au kama mtoto wa paa juu ya milima ya manukato."[c]

ISAYA

1 Maono[a] ya Isaya[b] mwana wa Amozi aliyoyaona kuhusu Yuda na Yerusalemu katika siku za Uzia,[c] Yothamu,[d] Ahazi[e] na Hezekia,[f] wafalme wa Yuda:[g]

2 Sikieni,[h] enyi mbingu, utege sikio, Ee dunia, kwa maana Yehova mwenyewe amesema: "Nimelea na kukuza wana,[i] lakini wao wenyewe wameniasi.[j] **3** Ng'ombe anamjua vema mnunuzi wake, na punda anaijua hori ya bwana wake; Israeli mwenyewe hakujua,[k] watu wangu mwenyewe hawakujiendesha kwa uelewaji."[l]

4 Ole wake taifa lenye dhambi,[m] watu walio na kosa zito, uzao unaotenda maovu,[n] wana wenye kuharibu![o] Wamemwacha Yehova,[p] wamemvunjia heshima Mtakatifu wa Israeli,[q] wamegeuka kuelekea nyuma.[r] **5** Ni wapi pengine mtakapopigwa tena,[s] kwa kuwa mnazidisha maasi?[t] Kichwa chote kimo katika hali ya ugonjwa, na moyo wote ni mnyonge.[a] **6** Kuanzia wayo wa mguu mpaka kwenye kichwa hakuna mahali pasipo na kasoro.[b] Majeraha na machubuko na mapigo ya hivi karibuni—hayakufinywa yatoe usaha wala kufungwa, wala kulainishwa kwa mafuta.[c] **7** Nchi yenu ni ukiwa,[d] majiji yenu yameteketezwa kwa moto;[e] udongo wenu—mbele ya macho yenu wageni[f] wanaula,[g] na ukiwa huo ni kama maangamizi yaliyofanywa na wageni.[h] **8** Na binti Sayuni[i] ameachwa akiwa amebaki kama kibanda katika shamba la mizabibu, kama kijumba cha mlinzi ndani ya shamba la matango, kama jiji lililozingirwa.[j] **9** Kama Yehova wa majeshi hangalituachia waokokaji wachache tu,[k] tungalikuwa kama Sodoma, tungalifanana na Gomora.[l]

SURA 1

a Hes 12:6
Ayu 33:15
Amo 3:7
b 2Nya 32:32
c 2Nya 26:22
Isa 6:1
d 2Nya 27:1
e 2Nya 28:1
f 2Fa 19:2
2Nya 29:1
2Nya 32:20
g Mt 1:9
h Zb 50:4
i Kum 1:31
Eze 16:13
j Kum 4:25
Isa 30:9
Eze 20:8
k Ho 4:6
l Kum 32:28
Zb 32:9
Ro 1:28
m Da 9:11
Mdo 7:51
n Hes 32:14
Amu 2:19
o Mik 7:2
p Kum 31:16
Ebr 3:10
q Kum 32:19
Yer 7:19
Yer 50:29
1Ko 10:22
r Zb 58:3
Yer 2:5
Yer 15:6
Ro 8:7
s Yer 2:30
Yer 5:3
t Yer 9:3

Safu ya 2

a Ne 9:34
Da 9:8
b Zb 38:3
c Lu 10:34
d Kum 28:63
Yer 44:2

e Isa 34:9; Yer 2:15; f 2Fa 10:32; g Kum 28:33; h 2Fa 18:11; Omb 5:2; i Isa 8:18; Zek 9:9; j 2Fa 18:14; Isa 5:2; Isa 8:8; Yer 4:17; Lu 19:43; k 2Fa 25:11; Omb 3:22; Ro 9:27; l Mwa 19:24; Kum 29:23; Amo 4:11; Ro 9:29.

10 Sikieni neno la Yehova,[a]
enyi madikteta[b] wa Sodoma.[c]
Tegeni sikio kwa sheria ya Mungu wetu, ninyi watu wa Gomora. **11** "Dhabihu zenu nyingi zina faida gani kwangu?"
asema Yehova. "Nimetosheka
na matoleo mazima ya kuteketezwa[d] ya kondoo-dume[e] na
mafuta ya wanyama walioli-
shwa vizuri;[f] nami sikupende-
zwa na damu[g] ya ng'ombe-dume wachanga na wana-kondoo
na mbuzi-dume.[h] **12** Ninyi
mnapoendelea kuingia ili kuona
uso wangu,[i] ni nani ambaye ame-
taka hilo kutoka mkononi
mwenu, kuzikanyaga-kanyaga
nyua zangu?[j] **13** Acheni kule-
ta ndani matoleo zaidi ya nafa-
ka yasiyo na thamani.[k] Uvumba
—ni chukizo kwangu.[l] Mwezi
mpya[m] na sabato,[n] kuita mkusa-
nyiko[o]—siwezi kuvumilia matu-
mizi ya nguvu za uchawi[p] pamo-
ja na kusanyiko kuu. **14** Nafsi
yangu imechukia miezi yenu mi-
pya na majira yenu ya sherehe.[q] Zimekuwa mzigo kwangu;[r]
nimechoka kuzibeba.[s] **15** Na-
nyi mnaponyoosha mikono
yenu,[t] mimi huficha macho ya-
ngu kutoka kwenu.[u] Hata mja-
potoa sala nyingi,[v] mimi sisikili-
zi;[w] mikono yenu imejaa umwa-
gaji wa damu.[x] **16** Jiosheni;[y] ji-
safisheni;[z] ondoeni ubaya wa
matendo yenu mbele za macho
yangu;[a] acheni kutenda maba-
ya.[b] **17** Jifunzeni kutenda
mema;[c] tafuteni haki;[d] mreke-
bisheni mkandamizaji;[e] fanye-
ni hukumu kwa ajili ya mvula-
na asiye na baba;[f] teteeni ma-
silahi ya mjane."[g]
18 "Sasa, njooni, nasi tunyo-
oshe mambo kati yetu," asema
Yehova.[h] "Hata dhambi zenu
zikiwa nyekundu, zitafanywa
kuwa nyeupe kama theluji;[a]
hata zikiwa nyekundu kama
kitambaa chekundu; zitaku-
wa kama sufu. **19** Ninyi mki-
onyesha utayari na kusikiliza, mtakula mema ya nchi.[b]
20 Lakini mkikataa[c] na kwa
kweli muwe waasi, mtaliwa na
upanga; kwa maana kinywa
cha Yehova kimesema hayo."[d]
21 Lo! Jinsi mji mwaminifu[e]
umekuwa kahaba![f] Uliku-
wa umejaa haki;[g] uadilifu uli-
kuwa ukikaa ndani yake,[h] la-
kini sasa ni wauaji.[i] **22** Fe-
dha yako imekuwa takataka.[j]
Pombe yako ya ngano imecha-
nganywa na maji.[k] **23** Wa-
kuu wako ni wakaidi na rafi-
ki za wezi.[l] Kila mmoja wao
ni mwenye kupenda rushwa[m]
na mwenye kufuatilia zawadi.[n]
Hawamtendei hukumu mvula-
na asiye na baba; na hata kesi
ya mjane haiwafikii.[o]
24 Kwa hiyo Bwana wa kwe-
li, Yehova wa majeshi, Mwe-
nye Nguvu wa Israeli,[p] asema hivi: "Aha! Nitajiondolea
wapinzani wangu, nitajilipi-
zia kisasi[q] juu ya adui zangu.[r]
25 Nami nitaugeuza mkono wa-
ngu juu yako, nitayeyusha ta-
kataka yako kana kwamba kwa
sabuni, nitaondoa uchafu wako
wote.[s] **26** Nami nitawarudi-
sha tena waamuzi kwa ajili yako
kama hapo kwanza, na washau-
ri kwa ajili yako kama pale
mwanzoni.[t] Kisha wewe uta-
itwa Jiji la Uadilifu, Mji Mwa-

SURA 1

a Amo 3:1
b Isa 3:6
c Mwa 13:13
Kum 32:32
Isa 3:9
Omb 4:6
Yud 7
d Ho 6:6
e Kut 29:38
Hes 29:39
Mik 6:7
f Law 3:16
g Law 4:18
Law 17:11
h Law 16:5
1Sa 15:22
Zb 40:6
Zb 51:16
Met 15:8
Mt 9:13
i Kut 23:17
Kum 16:16
j Mhu 5:1
Mal 1:8
k Mal 2:12
Lu 11:42
l Met 15:9
Met 21:27
Eze 8:11
m Hes 28:11
n Kut 31:13
o Law 23:2
Zb 81:3
p Law 19:26
1Sa 15:23
q Amo 5:21
Amo 8:5
r Isa 43:24
s Mal 2:17
t 1Fa 8:22
Ezr 9:5
u Met 15:29
v Mt 6:7
w Met 28:9
Isa 59:2
Omb 3:44
Mik 3:4
x Isa 59:3
Yer 7:9
Mik 3:2
y Zb 26:6
Yer 4:14
Mdo 22:16
Ufu 7:14
z 1Ko 5:8
2Ko 7:1
a Isa 55:7
Eze 18:30
1Pe 2:1
b Zb 34:14
1Pe 3:11
c Amo 5:15
Mik 6:8
d Zb 82:3
Zb 112:5
e Met 31:9
f Yer 22:3
g Kum 10:18
h Yer 2:5
Ho 14:1
Mik 6:2
Yak 4:8

Safu ya 2

a Zb 51:7
Isa 44:22
Omb 4:7
Mik 7:19
b Kum 28:2
Yoe 2:26
c 1Sa 12:25
Met 29:1
Da 9:5
Ho 13:16

d Law 26:33; Kum 28:15; Kum 30:19; 1Sa 15:29; 2Pe 3:9; e Zb 48:2; Zek 8:3; f Yer 2:20; Yer 3:6; Eze 16:22; g 2Sa 8:15; 1Fa 3:28; h 2Nya 19:9; 2Nya 19:10; i Mik 3:3; Lu 13:34; Mdo 7:52; j Omb 4:1; Eze 22:18; k Ho 4:18; l Isa 3:14; Mik 3:9; m Kut 23:8; Met 17:23; n Met 21:14; Mhu 7:7; o Kut 22:22; Yer 5:28; Mal 3:5; Lu 18:3; p Isa 60:16; q Eze 25:14; Ho 8:3; Ro 12:19; r Kum 32:43; Isa 59:18; Eze 5:13; s Yer 6:29; Yer 9:7; Mal 3:3; t Hes 12:3; 1Sa 12:3; Isa 32:1; Eze 34:23.

minifu.[a] **27** Sayuni atakombolewa kwa haki,[b] na watu
wake wanaorudi, kwa uadilifu.[c] **28** Na anguko la waasi na
la wenye dhambi litakuwa kwa
wakati uleule mmoja,[d] na wale
wanaomwacha Yehova watafikia mwisho wao.[e] **29** Kwa maana wataona aibu kwa sababu
ya miti yenye nguvu ambayo
ninyi mliitamani,[f] nanyi mtafedheheka kwa sababu ya bustani ambazo mmechagua.[g]
30 Kwa maana mtakuwa kama
mti mkubwa ambao majani yake
yananyauka,[h] na kama bustani ambayo haina maji. **31** Na
mwanamume mwenye nguvu
kwa hakika atakuwa kitani,[i] na
matunda ya kazi yake yatakuwa cheche; na vyote viwili hakika vitateketezwa katika miali ya moto kwa wakati uleule
mmoja, bila kuwa na yeyote wa
kuzima."[j]

2 Jambo ambalo Isaya mwana wa Amozi aliona katika maono kuhusu Yuda na
Yerusalemu:[k] **2** Na itatukia
katika siku za mwisho[l] kwa-
mba mlima wa nyumba[m] ya Yehova utawekwa imara juu ya
kilele cha milima,[n] nao utainuliwa juu ya vilima;[o] na mataifa yote yatamiminika huko.[p]
3 Na vikundi vingi vya watu
hakika vitaenda na kusema:
"Njooni,[q] twendeni juu kwenye mlima wa Yehova, kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo; naye atatufundisha njia
zake, nasi tutatembea katika
mapito yake."[r] Kwa maana sheria itatoka katika Sayuni, na
neno la Yehova katika Yerusalemu.[s] **4** Naye hakika atafanya hukumu kati ya mataifa[t]
na kunyoosha mambo[u] kuhusu
vikundi vingi vya watu.[a] Nao
watafua panga zao ziwe majembe na mikuki yao iwe miundu.[b] Taifa halitainua upanga
juu ya taifa, wala hawatajifunza vita tena.[c]

5 Enyi watu wa nyumba ya
Yakobo, njooni tutembee katika nuru ya Yehova.[d]

6 Kwa maana umewaacha
watu wako, nyumba ya Yakobo.[e] Kwa maana wamejaa vitu
vya kutoka Mashariki,[f] nao ni
wenye kufanya uchawi[g] kama
Wafilisti, nao wamejawa na
wana wa wageni.[h] **7** Na nchi
yao imejaa fedha na dhahabu,
na hakuna kikomo kwa hazina
zao.[i] Na nchi yao imejaa farasi, na hakuna kikomo kwa magari yao.[j] **8** Na nchi yao imejaa miungu isiyo na thamani.[k]
Wao huinamia kazi ya mikono ya mtu, kile ambacho vidole vya mtu vimetengeneza.[l]
9 Na mtu wa udongo huinama,
na mwanadamu hushuka, nawe
huwezi kuwasamehe.[m]

10 Ingia ndani ya mwamba,
ujifiche katika mavumbi kwa
sababu ya hofu ya Yehova, na
kutoka mbele ya ukuu wake
wa fahari.[n] **11** Macho yenye
majivuno ya mtu wa udongo yatashushwa, na kiburi cha wanadamu kitainama;[o] na Yehova
peke yake atainuliwa juu siku
hiyo.[p] **12** Kwa maana hiyo ni
siku ya Yehova wa majeshi.[q]
Iko juu ya kila mtu aliyejikweza na aliye juu sana na juu

SURA 1
a Isa 62:1 Zek 8:8
b Kum 24:18 Yer 31:11
c 1Ko 1:30 2Ko 5:21
d Zb 1:6 Zb 37:38 Zb 104:35 Met 29:1 Eze 20:38 2Pe 3:7
e 1Sa 12:25 1Fa 9:6 2Th 1:9
f Yer 2:20 Yer 3:6 Eze 6:13 Ho 4:13 Ro 6:21
g Isa 65:3 Isa 66:17
h Yer 17:6 Eze 17:9 Mt 21:19
i Eze 32:21
j Zb 73:27 Isa 34:10 Eze 20:47 Mal 4:1

SURA 2
k Isa 1:1 Mik 1:1 Hab 1:1
l Yer 23:20 Yer 30:24 Eze 38:16 Da 12:9 Mdo 2:17 2Ti 3:1 Ufu 12:12
m Mdo 10:35 1Pe 2:5
n Da 2:35 Zek 8:3 Ebr 12:22 Ufu 21:10
o Mik 4:1
p Zb 2:8 Zb 72:8 Zb 86:9 Hag 2:7 Mal 3:12 Ufu 11:15
q Yer 31:6 Zek 8:23 Ufu 22:17
r Zb 25:8 Isa 54:13 Mik 4:2 Yoh 7:16 Mdo 10:33 1Th 4:9
s Zb 110:2 Isa 51:4 Ro 10:18 Ufu 21:24
t 1Sa 2:10 Zb 82:8 Zb 96:13 Zb 110:6 Mdo 17:31
u Met 11:5 Mt 3:3 Lu 3:5 Yoh 1:23 2Ti 3:16 Ebr 9:10

Safu ya 2
a Isa 1:18 Efe 2:1 Kol 2:13

b Zb 46:9; Ho 2:18; Zek 9:10; c Zb 72:7; Isa 60:18; Mik 4:3; Mt 5:44; Mt 26:52; d Zb 89:15; Isa 60:19; 1Yo 1:7; Ufu 21:23; e Kum 31:17; 2Nya 24:20; f Ufu 17:5; g Law 19:31; Kum 18:10; Zb 106:35; h Ezr 9:2; Ne 13:24; i 1Fa 10:21; j Kum 17:16; 1Fa 4:26; k 2Nya 28:2; 2Nya 33:7; Yer 2:28; l Kum 4:28; Zb 115:4; Ho 13:2; Ufu 9:20; m Kut 20:7; Yos 24:19; Yer 18:23; Mk 3:29; n Kut 20:18; 1Nya 29:11; Zb 119:120; o Yer 50:32; Mal 4:1; Lu 18:14; Yak 4:6; 1Pe 5:5; p Isa 24:23; Mik 4:7; Sef 2:11; q Isa 13:6; Yer 46:10; Eze 13:5; Amo 5:18; 1Th 5:2.

ya kila mtu aliyejiinua juu au
aliye chini;[a] **13** na juu ya mi-
erezi yote ya Lebanoni[b] amba-
yo ni mirefu na iliyoinuliwa
juu na juu ya miti yote miku-
bwa sana ya Bashani;[c] **14** na
juu ya milima yote mirefu na
juu ya vilima vyote ambavyo vi-
meinuliwa juu;[d] **15** na juu ya
kila mnara mrefu na juu ya kila
ukuta wenye ngome;[e] **16** na
juu ya meli zote za Tarshi-
shi[f] na juu ya mashua zote ze-
nye kutamanika. **17** Na maji-
vuno ya mtu wa udongo yatai-
nama, na kiburi cha wanadamu
kitashushwa;[g] na Yehova peke
yake atainuliwa juu katika siku
hiyo.[h]

18 Na miungu isiyo na tha-
mani itapitilia mbali kabisa.[i]
19 Na watu wataingia ndani ya
mapango ya miamba na ndani
ya mashimo ya mavumbi kwa
sababu ya hofu ya Yehova na
kutoka mbele ya ukuu wake
wenye fahari,[j] atakaposimama
ili dunia ipatwe na mitetemeko.[k]
20 Katika siku hiyo mtu
wa udongo atatupia panya-sa-
nge na popo miungu yake ya
fedha ya ubatili na miungu
yake ya dhahabu isiyo na tha-
mani ambayo walikuwa wame-
mfanyia yeye ili ainame mbe-
le yake,[l] **21** ili aingie ndani
ya mashimo katika miamba na
ndani ya mipasuko ya miamba,
kwa sababu ya hofu ya Yehova
na kutoka mbele ya ukuu wake
wenye fahari,[m] atakaposima-
ma ili dunia ipatwe na mitete-
meko. **22** Kwa ajili yenu we-
nyewe, jiepusheni kutoka kwa
mtu wa udongo, ambaye pumzi
yake iko katika mianzi ya pua
yake,[n] kwa sababu yeye atafiki-
riwa kwa msingi gani?[o]

SURA 2

a Isa 66:16; Yer 25:31
b Isa 10:33; Eze 31:3; Zek 11:2
c Amo 4:1
d Zb 110:5
e Sef 1:16
f 1Fa 10:22; Eze 27:25
g Isa 13:11; Yer 48:29; Eze 28:5
h Isa 2:11
i Isa 27:9; Eze 36:25; Eze 37:23; Ho 14:8; Zek 13:2
j Zb 76:7; Isa 2:10; Lu 23:30; 2Th 1:9; Ufu 6:15
k Zb 7:6; Mik 1:3; Ebr 12:26; 2Pe 3:10; Ufu 16:18
l Isa 2:8; Isa 30:22; Isa 31:7
m 1Nya 29:11; Zb 96:6; Zb 119:120
n Mwa 2:7; Ayu 27:3
o Ayu 7:17; Zb 8:4

Safu ya 2

SURA 3

a Isa 37:20; Isa 44:6; Yer 10:10
b 2Fa 23:27; 2Nya 36:19
c Law 26:26; Kum 28:51; Yer 37:21; Eze 4:16
d Eze 13:9
e 2Fa 24:14; Zb 74:9; Omb 5:12
f Kut 18:21; Kum 1:15; 1Sa 8:12
g Kum 18:10; Zb 58:5; Isa 8:19
h Amu 21:25; Mhu 10:16
i Isa 9:19; Yer 9:5; Mik 3:3; Mal 3:5
j Ayu 30:1
k Law 19:32; 2Sa 16:5; Met 16:31; Mhu 10:7; Mk 14:65
l Isa 1:10; Isa 22:3; Yoh 6:15
m 2Nya 28:5; 2Nya 28:18; 2Nya 33:11; Yer 26:18; Mik 3:12

3 Kwa maana, tazama![a] Bwa-
na wa kweli, Yehova wa ma-
jeshi, anaondoa katika Yerusa-
lemu[b] na katika Yuda kitege-
meo na tegemeo, kitegemeo ki-
zima cha mkate na kitegemeo
kizima cha maji,[c] **2** mwana-
mume mwenye nguvu na shu-
jaa wa vita, mwamuzi na na-
bii,[d] na mwaguzi na mwanamu-
me mzee,[e] **3** mkuu wa watu
50[f] na mwanamume mwenye
kuheshimiwa sana na mshau-
ri na mjuzi wa ufundi wa uchawi, na mchawi stadi.[g] **4** Nami
hakika nitawafanya wavula-
na kuwa wakuu wao, na ngu-
vu za kidhalimu zitatawa-
la juu yao.[h] **5** Na watu kwa
kweli wataoneana, kila mmoja
na mwenzake.[i] Watashambu-
lia, mvulana juu ya mwanamu-
me mzee,[j] na mwenye kupuuzwa juu ya mtu aliye wa kuhe-
shimiwa.[k] **6** Kwa maana kila
mmoja atamshika ndugu yake
ndani ya nyumba ya baba yake,
akisema: "Wewe una nguo ya
kujitanda. Unapaswa kuwa di-
kteta[l] kwetu, na hili rundo
la mabomoko lililoharibiwa li-
napasa kuwa chini ya mkono
wako." **7** Yeye atapaaza sauti
yake siku hiyo, akisema: "Mimi
sitakuwa mfunga-majeraha;
na nyumbani mwangu hamna
mkate wala nguo ya kujitanda.
Msiniweke kuwa dikteta juu ya
watu."

8 Kwa maana Yerusalemu li-
mejikwaa na Yuda imeangu-
ka,[m] kwa sababu ulimi wao na
matendo yao yanapingana na
Yehova,[n] katika kujiendesha
kwa uasi machoni pa utukufu
wake.[o] **9** Sura ya nyuso zao
kwa kweli hushuhudia dhidi

n Zb 73:8; Eze 9:9; Mal 3:13; Mt 12:36; Yud 15;
o 2Nya 33:6; Hab 1:13; Mal 2:2; 1Ko 10:22.

yao,[a] nazo zinaeleza kuhusu
dhambi yao kama ile ya Sodo-
ma.[b] Hawajaificha. Ole wa nafsi
yao! Kwa maana wamejiletea
wenyewe msiba.[c]
10 Semeni kwamba itakuwa
vema kwa mwadilifu,[d] kwa maa-
na watakula matunda ya ma-
tendo yao.[e] **11** Ole wake mtu
mwovu!—Msiba; kwa maana
matendo yaliyotendwa kwa mi-
kono yake mwenyewe atalipwa
yeye![f] **12** Na kuhusu watu
wangu, wagawa-kazi wao wa-
natenda vikali, na wanawake
kwa kweli hutawala juu yao.[g]
Enyi watu wangu, wale wanao-
waongoza wanawapoteza ni-
nyi,[h] nao wameivuruga njia ya
mapito yenu.[i]
13 Yehova anasimama ili ku-
shindana, naye amesimama ili
kukata hukumu juu ya vikundi
vya watu.[j] **14** Yehova mwe-
nyewe ataingia katika hukumu
pamoja na wazee wa watu wake
na wakuu wao.[k]
"Nanyi wenyewe mmeliteke-
teza kwa moto shamba la ni-
zabibu. Vitu vilivyochukuliwa
kwa unyang'anyi kutoka kwa
mwenye kuteseka vimo nda-
ni ya nyumba zenu.[l] **15** Ninyi
mnamaanisha nini kwa kuwa
mnawaponda watu wangu, na
kwa kuwa mnazisaga nyuso
za wenye kuteseka?"[m] asema
Bwana Mwenye Enzi Kuu, Ye-
hova wa majeshi.
16 Na Yehova anasema:
"Kwa sababu binti za Sayuni
wamekuwa na majivuno, nao
wanatembea shingo zao ziki-
wa zimenyooshwa na kutupa
macho yao kwa kutamani, wa-
natembea kwa hatua fupifu-
pi, na kwa miguu yao wana-
toa milio ya kengele,[n] **17** Ye-

SURA 3
a Zb 73:6; Met 30:13; 1Ti 5:24
b Mwa 18:20; Isa 1:10; Yud 7
c Omb 3:64; Ho 13:9
d Zb 18:24; Zb 128:1; Mhu 8:12; Sef 2:3; Ro 2:10
e Zb 128:2; Ga 6:7; Ebr 6:10
f Zb 28:4; Zb 62:12; 2Ko 5:10; 2Ti 4:14; Yak 2:13
g 2Fa 11:1; Nah 3:13; 1Ti 2:12
h Isa 9:16
i Yer 5:31; Hab 1:4; Mt 15:14; Mt 23:15
j Zb 12:5; Met 22:23; Ho 4:1; Mik 6:2
k Yer 12:10; Lu 12:48; Yak 3:1
l Isa 1:23; Yer 5:27; Amo 4:1; Mik 2:2; Mik 6:10
m Isa 58:4; Amo 2:6; Amo 8:4; Mik 3:2
n Kum 8:14; Isa 32:9; Eze 16:49

Safu ya 2
a Kum 28:27
b Isa 3:24; 1Ko 11:6
c Amu 8:26
d Mwa 24:22; Kut 32:2; Eze 16:11; Ho 2:13
e Yer 2:32
f Kut 35:22; Hes 31:50
g Mwa 24:22
h Kut 38:8
i Law 16:4
j Mwa 38:14; Isa 47:2
k Est 2:12
l Isa 22:12; Eze 7:18; Mik 1:16
m Yer 4:8; Omb 2:10; Yoe 1:8; Amo 8:10
n Ga 6:17
o 2Nya 29:9; Yer 11:22; Omb 2:21; Amo 9:10
p Yer 14:2; Omb 1:4
q Ayu 2:13; Isa 47:1; Omb 2:10

hova pia atafanya utosi wa bi-
nti za Sayuni kuwa na vigaga,[a]
na Yehova mwenyewe atafunua
wazi paji la uso wao.[b] **18** Ka-
tika siku hiyo Yehova ataoondolea mbali uzuri wa bangili na tepe za kichwani na mapambo yenye umbo la mwezi,[c] **19** herini na vikuku na shungi,[d] **20** vitambaa vya kichwani na mafurungu na mavazi ya kifuani[e] na 'nyumba za nafsi' na kauri zenye kuvuma za mapambo,[f] **21** pete za vidole na pete za pua,[g] **22** na kanzu za fahari na kanzu fupi za nje na kanzu na vikoba, **23** na vioo vya mkononi[h] na mavazi ya ndani na vilemba[i] na shungi[j] kubwa.
24 "Na itatukia kwamba badala ya mafuta ya zeri[k] kutakuwa na harufu tupu ya kuoza; na badala ya mshipi, kamba; na badala ya nywele zilizosukwa kwa mpangilio wa usanii, upara;[l] na badala ya vazi lenye thamani, kuvaa nguo za magunia;[m] kutiwa alama[n] mwilini badala ya urembo. **25** Wanaume wako wataanguka kwa upanga, na nguvu zako kwa vita.[o] **26** Na milango yake italazimika kuomboleza na kuhuzunika,[p] naye hakika ataachwa ukiwa. Atakaa chini kwenye udongo."[q]

4 Na wanawake saba kwa kweli watamkamata mwanamume mmoja siku hiyo,[r] wakisema: "Tutakula mkate wetu wenyewe na kuvaa nguo zetu wenyewe; ila tu sisi na tuitwe kwa jina lako ili kuiondoa shutuma yetu."[s]
2 Katika siku hiyo kile ambacho Yehova anachipusha[t]

SURA 4 r Isa 3:25; s Mwa 30:23; Isa 54:4; Lu 1:25; t Isa 27:6; Isa 60:21; Yoe 2:18.

kitakuwa kwa ajili ya pambo
na kwa ajili ya utukufu,[a] na
mazao ya nchi yatakuwa kitu
cha kujivunia[b] na kitu kizu-
ri kwa ajili ya wale wa Israe-
li walioponyoka.[c] **3** Na itatu-
kia kwamba wale waliobaki ka-
tika Sayuni na wale waliosalia
katika Yerusalemu watasemwa
kuwa ni watakatifu kwake,[d]
kila mtu aliyeandikwa kwa aji-
li ya uzima katika Yerusalemu.[e]
4 Yehova atakapokuwa
ameosha kinyesi cha binti za
Sayuni[f] naye atausafisha[g]
umwagaji wa damu[h] wa Yeru-
salemu kutoka ndani yake kwa
roho ya hukumu na kwa roho
ya kuteketeza,[i] **5** pia juu ya
kila mahali palipofanywa ima-
ra pa Mlima Sayuni[j] na juu ya
mahali pake pa mkusanyiko
hakika Yehova ataumba wingu
wakati wa mchana na moshi,
na mwangaza wa moto unao-
waka[k] wakati wa usiku;[l] kwa
sababu kutakuwa na kificho
juu ya utukufu wote.[m] **6** Na
kutakuwa na kibanda kwa aji-
li ya kivuli wakati wa mcha-
na kutokana na joto kavu,[n] na
kwa ajili ya kimbilio na kwa aji-
li ya maficho kutokana na dho-
ruba na kutokana na mvua.[o]

5 Tafadhali, acha nimwimbie
mpenzi wangu wimbo wa
mpenzi wangu kuhusu sha-
mba lake la mizabibu.[p] Pali-
kuwa na shamba la mizabibu
ambalo mpenzi wangu aliku-
wa nalo kando ya kilima che-
nye kuzaa sana. **2** Naye aka-
lilima na kuliondoa mawe na
kulipanda mzabibu bora mwe-
kundu, na kujenga mnara kati-
kati yake.[q] Na pia kulikuwa na
shinikizo la divai ambalo ali-
chimba ndani yake.[r] Naye aka-

SURA 4

a Zek 9:17
b Isa 30:23
Yoe 3:18
c Isa 10:20
Isa 66:19
Yer 44:14
Eze 7:16
d Isa 60:21
Zek 14:5
Mt 23:35
e Kut 32:32
Ufu 3:5
Ufu 20:15
f Eze 22:15
Eze 36:25
g Eze 16:9
h Eze 24:7
i Eze 22:20
Mal 3:2
Mt 3:12
j Zb 87:2
Isa 32:18
Isa 33:20
Isa 37:35
k Kut 13:21
Hes 9:15
Zek 2:5
l Kut 40:38
m Zb 85:9
n Zb 91:1
Zb 121:5
o Isa 25:4
Isa 32:2

SURA 5

p Zb 80:8
Isa 5:7
Yer 2:21
Lu 20:9
q Mk 12:1
r Mt 21:33

Safu ya 2

a Ho 9:10
1Ko 9:7
b Isa 5:7
Yer 2:21
Ho 10:1
c Yer 2:5
Mik 6:2
d 2Nya 36:15
Eze 24:13
Mdo 7:51
e Ayu 1:10
f Law 26:31
Kum 28:63
Ne 2:3
Zb 79:1
Omb 2:7
g Isa 26:6
Omb 1:15
h Law 26:33
Yer 25:11
i Kum 29:23
Yer 45:4
j Isa 7:23
Isa 32:13
Ebr 6:8
k Kum 11:17
Kum 28:23
Amo 4:7
l Zb 80:8
Yer 12:10
Lu 20:9
m Kut 15:17
Zb 147:11
Zb 149:4
n Yer 22:15
Mik 6:8
Zek 7:9
o Mwa 19:13
Kum 15:9
Ayu 34:28
Lu 18:7

endelea kulitumaini lizae zabi-
bu,[a] lakini mwishowe likazaa
zabibu-mwitu.[b]
3 "Na sasa, enyi wakaaji wa
Yerusalemu nanyi watu wa
Yuda, tafadhali hukumuni kati
yangu na shamba langu la mi-
15 Tangazo juu ya Moabu:[c] Kwa sababu limeporwa wakati wa usiku, Ari[d] la Moabu limenyamazishwa. Kwa sababu limeporwa wakati wa usiku, Kiri[e] la Moabu limenyamazishwa. **2** Ameenda mpaka juu kwenye Ile Nyumba na mpaka Diboni,[f] mpaka mahali pa juu, kwenye kilio. Moabu inapiga mayowe juu ya Nebo[g] na juu ya Medeba.[h] Pana upara[i] juu ya vichwa vyote ndani yake; ndevu zote zimenyolewa. **3** Wamevaa nguo za magunia[j] katika barabara zake. Katika madari[k] ya huko na katika viwanja vya watu wote vya huko kila mtu huko analia, anashuka huku akilia.[l] **4** Na Heshboni na Eleale[m] yanalia. Sauti yao imesikika mpaka Yahazi.[n] Ndiyo sababu watu wenye silaha wa Moabu wanaendelea kupaaza sauti. Nafsi yake imetetemeka ndani yake.

5 Moyo wangu unamlilia Moabu mwenyewe.[o] Wakimbizi wa huko wamefika mbali mpaka Soari[p] na Eglath-shelishiya.[q] Kwa maana kwenye mpando wa Luhithi[r]—kila mmoja anaupanda akilia; kwa maana katika njia ya kwenda Horonaimu[s] wanapaaza kilio kuhusu ule msiba. **6** Kwa maana maji ya Nimrimu[t] yanakuwa ukiwa mtupu. Kwa maana majani mabichi yamenyauka,

q Yer 48:34; r Yer 48:5; s Yer 48:3; t Yer 48:34.

majani yamefika mwisho; hakuna chochote ambacho kimekuwa kijani kibichi.[a] **7** Ndiyo sababu masalio na mali zao zilizowekwa ghalani ambazo wameweka, wanaendelea kuzibeba na kuzivusha kwenye bonde la mto la mierebi. **8** Kwa maana kilio kimezunguka eneo la Moabu.[b] Mayowe ya huko yamefika mpaka Eglaimu; mayowe ya huko yamefika mpaka Beer-elimu, **9** kwa sababu maji ya Dimoni yamejaa damu. Kwa maana nitaweka vitu zaidi juu ya Dimoni, kama vile simba kwa ajili ya wale wa Moabu watakaoponyoka na kwa ajili ya mabaki wa nchi hiyo.[c]

16 Pelekeni kondoo-dume kwa mtawala wa nchi,[d] kutoka Sela kuelekea nyikani, kwenye mlima wa binti Sayuni.[e]

2 Na itatukia kwamba, kama vile kiumbe chenye mabawa kinachokimbia, kilichofukuzwa kutoka katika kiota chake,[f] ndivyo watakavyokuwa binti za Moabu kwenye vivuko vya Arnoni.[g]

3 "Leteni shauri, tekelezeni uamuzi.[h]

"Fanya kivuli chako kama usiku katikati ya mchana.[i] Wafiche waliotawanywa;[j] usimsaliti yeyote anayekimbia.[k] **4** Watu wangu waliotawanywa na wakae wakiwa kama wageni ndani yako, Ee Moabu.[l] Uwe maficho kwao kwa sababu ya mporaji.[m] Kwa maana mkandamizaji ameufikia mwisho wake; uporaji umekoma; wale wanaowakanyaga wengine wamemalizwa kutoka duniani.[n]

SURA 15
a Isa 16:9
Hab 3:17
b Yer 48:20
c Law 26:22
2Fa 17:25
Yer 15:3
Amo 5:19

SURA 16
d Ezr 7:17
e Isa 10:32
Mik 4:8
f Met 27:8
Isa 13:14
Yer 48:19
g Hes 21:13
h Zb 82:3
Isa 1:17
Yer 21:12
Da 4:27
Zek 7:9
i Kum 28:29
j Isa 32:2
k Oba 14
l 1Sa 22:3
m Yer 48:8
Yer 48:42
n Isa 33:1

Safu ya 2
a Zb 45:6
Zb 89:14
Met 20:28
b 2Sa 7:16
Isa 9:7
Yer 23:5
Da 7:14
c Zb 72:2
Isa 32:1
d Yer 48:26
Yer 48:29
Sef 2:10
e Amo 2:1
f Yer 48:7
g Isa 15:2
Yer 48:20
h 2Fa 3:25
i Yos 13:17
j Hes 32:38
Yos 13:19
k Hes 32:3
Yos 13:25
Yer 48:32
l Yer 48:32
m Isa 15:4
n Yer 48:34
o Amu 9:27
p Isa 24:8
Yer 25:30
Yer 48:33
q Hab 3:17
r Sef 2:9

5 "Na kiti cha ufalme hakika kitafanywa imara kwa fadhili zenye upendo;[a] na mtu ataketi juu yake katika ukweli ndani ya hema la Daudi,[b] akihukumu na kutafuta haki na kuwa mwenye haraka kufanya uadilifu."[c]

6 Tumesikia juu ya kiburi cha Moabu, kwamba yeye ana kiburi sana;[d] majivuno yake na kiburi chake na ghadhabu yake[e]—maneno yake matupu hayatakuwa hivyo.[f] **7** Kwa hiyo Moabu atampigia mayowe Moabu; naam, yote itapiga mayowe.[g] Waliopigwa wataomboleza kwa sababu ya keki za zabibu kavu za Kir-haresethi,[h] **8** kwa sababu matuta ya Heshboni[i] yamenyauka. Mzabibu wa Sibma[j]—wamiliki wa mataifa wamekata matawi yake mekundu. Wamefika mpaka Yazeri;[k] walikuwa wametangatanga nyikani. Machipukizi yake yalikuwa yameachwa yatoe majani; yalikuwa yamevuka mpaka baharini.

9 Hiyo ndiyo sababu nitalia kwa kilio cha Yazeri juu ya mzabibu wa Sibma.[l] Nitakulowesha wewe kwa machozi yangu, Ee Heshboni[m] na Eleale,[n] kwa sababu kupaaza sauti kumeanguka juu ya kiangazi chako na juu ya mavuno yako.[o] **10** Na kushangilia na shangwe zimeondolewa katika shamba la matunda; na hakuna vigelegele vya shangwe katika mashamba ya mizabibu, hakuna sauti inayopaazwa.[p] Mwenye kukanyaga hakanyagi divai yoyote itoke katika mashinikizo.[q] Nimekomesha kupaaza sauti.[r]

11 Ndiyo sababu matumbo
yangu yana msukosuko kama
kinubi juu ya Moabu,[a] na sehe-
mu yangu ya ndani juu ya Kir-
haresethi.[b]
12 Na ikatukia kwamba ili-
onekana kuwa Moabu alicho-
shwa akiwa juu ya mahali pa
juu;[c] naye akaja katika patakatifu pake kusali,[d] naye haku-
weza kutimiza lolote.[e]
13 Hili ndilo neno ambalo
Yehova alisema kuhusu Moa-
bu hapo zamani. **14** Na sasa
Yehova amesema hivi: "Katika muda wa miaka mitatu,
kulingana na miaka ya mfanya-
kazi wa kukodiwa,[f] utukufu[g]
wa Moabu utafedheheshwa pia
kwa fujo nyingi za kila aina, na
wale watakaobaki watakuwa
wachache mno, wasio na ngu-
vu."[h]

17 Tangazo juu ya Dama-
sko:[i] "Tazama! Damasko
limeondolewa lisiwe jiji, nalo li-
mekuwa rundo, bomoko linalo-
haribika.[j] **2** Majiji ya Aroeri[k]
ambayo yameachwa yameku-
wa mahali pa makundi, amba-
po kwa kweli yanajilaza, pasi-
po mtu yeyote wa kuyatetemesha.[l] **3** Na jiji lenye ngome li-
mekomeshwa kutoka katika
Efraimu,[m] na ufalme kutoka
katika Damasko;[n] na wale wa-
liobaki wa Siria watakuwa tu
kama utukufu wa wana wa
Israeli," asema Yehova wa ma-
jeshi.[o]
4 "Na itatukia katika siku
hiyo kwamba utukufu wa Yako-
bo utakuwa wa hali ya chini,[p]
na hata unono wa nyama yake
utakondeshwa.[q] **5** Na itatu-
kia kwamba mvunaji anapoku-
sanya nafaka inayosimama na
mkono wake unapovuna masu-
ke ya nafaka,[a] atakuwa kama
mtu anayeokota masalio ya ma-
suke ya nafaka katika nchi ta-
mbarare ya chini ya Refaimu.[b]
6 Na lazima ndani yake paba-
ki masalio kama kunapokuwa
na upigaji wa mzeituni: zeitu-
ni mbili au tatu zilizoiva juu ya
tawi; nne au tano juu ya mata-
wi yanayozaa matunda hapo,"
asema Yehova Mungu wa Isra-
eli.[c]
7 Katika siku hiyo mtu wa
udongo atatazama juu kwa
Mtengenezaji wake, na macho
yake yatamtazama Mtakatifu
wa Israeli.[d] **8** Naye hatazita-
zama madhabahu,[e] kazi ya mi-
kono yake;[f] naye hatatazama
kile ambacho vidole vyake vi-
metengeneza, kwenye miti mi-
takatifu wala kwenye vinara
vya uvumba.[g] **9** Katika siku
hiyo majiji yake yenye ngome
yatakuwa kama mahali pali-
poachwa kabisa katika mwi-
tu, hata lile tawi ambalo wa-
meliacha kabisa kwa sababu
ya wana wa Israeli; napo la-
zima pawe mahame yenye ukiwa.[h] **10** Kwa maana ume-
msahau[i] Mungu wa wokovu
wako;[j] nawe hukumkumbuka
Mwamba[k] wa ngome yako. Ndi-
yo sababu unapanda masha-
mba makubwa yenye kupende-
za, nawe unayaweka chipu-
kizi la mgeni. **11** Wakati wa
mchana unaweza kulijengea
ua shamba lako kwa uangali-
fu, nawe unaweza kuichipusha
mbegu yako wakati wa asubu-
hi, lakini hakika mavuno yata-
kimbia katika siku ya ugonjwa
na maumivu yasiyoweza ku-
ponywa.[l]

SURA 16
a Isa 15:5; Yer 48:36
b Isa 15:1
c Hes 22:41; Hes 23:1; Yer 48:35
d 1Fa 11:7; 2Fa 3:27; Yer 48:7
e 2Fa 19:18; Zb 115:4; Yer 10:5; Yer 16:20; 1Ko 8:4
f Isa 21:16
g Isa 23:9; Yer 9:23; Yer 48:46
h Isa 25:10; Yer 48:47; Sef 2:9

SURA 17
i 1Nya 18:5; Yer 49:23; Amo 1:5
j 2Fa 16:9; Isa 8:4; Zek 9:1
k Hes 32:34; Yos 13:16; 2Fa 10:33; Yer 48:19
l Sef 2:7
m 2Fa 17:6; Isa 7:8; Ho 5:14; Ho 9:13
n 2Fa 16:9
o Isa 28:2; Ho 9:11
p Isa 9:9; Isa 10:4
q Kum 32:15; Isa 10:16

Safu ya 2
a Kum 23:25; Yer 9:22; Ho 6:11; Yoe 3:13
b Yos 15:8; Yos 18:16; 2Sa 5:18
c Kum 4:27; Kum 24:20; Amu 8:2; Isa 24:13; Ro 9:27
d Isa 10:20; Isa 29:19; Mik 7:7
e 2Nya 31:1; 2Nya 34:7; Yer 17:2; Eze 36:25; Ho 8:11; Ho 14:8; Zek 13:2
f Isa 2:8; Ho 8:6; Mik 5:13
g 2Nya 34:4
h Isa 6:11; Ho 10:14; Amo 3:11; Mik 5:11; Mik 7:13
i Kum 6:12; Zb 50:22; Isa 1:3; Yer 2:32; Ho 8:14

j 1Nya 16:35; Zb 65:5; Zb 79:9; Hab 3:18; Ufu 7:10;
k Kum 32:4; 2Sa 22:32; Zb 18:2; Isa 26:4;
l Kum 28:30; Yer 12:13; Ho 8:7; Sef 1:13.

12 Lo, fujo za vikundi vingi
vya watu, ambao wana mchafu-
ko kama mchafuko wa bahari!
Nazo kelele za vikundi vya tai-
fa, wanaofanya kishindo kama
kelele za maji yenye nguvu![a]
13 Vikundi vya taifa[b] vitafa-
nya kishindo kama kelele za
maji mengi. Na Yeye atavike-
mea,[c] navyo vitakimbia na ku-
fukuzwa kama makapi ya mi-
lima mbele ya upepo na kama
mgurumo wa mbaruti mbele ya
upepo wa dhoruba.[d] **14** Wa-
kati wa jioni, kumbe, tazama!
kuna tisho la ghafula. Kabla
ya asubuhi—halipo tena.[e] Hilo
ndilo fungu la wale wanaotute-
ka, na kura ya wale wanaotu-
pora.[f]

18 Lo, nchi ya wadudu we-
nye kuvuma walio na
mabawa, iliyoko katika eneo
la mito ya Ethiopia![g] **2** Hiyo
ndiyo inayotuma wajumbe[h]
kwa njia ya bahari, na kwa
njia ya vyombo vya mafunjo
juu ya uso wa maji, ikisema:
"Nendeni, enyi wajumbe wepe-
si, kwa taifa lenye watu wa-
refu na walio laini, kwa watu
wenye kuogopesha kila mahali,
taifa lenye nguvu zinazodumu
na lenye kukanyaga-kanyaga,
ambalo mito imeifagilia mbali
nchi yake."[i]
3 Enyi wakaaji wote wa
nchi yenye kuzaa[j] nanyi wa-
kaaji wa dunia, mtaona mao-
no kama wakati ishara ina-
poinuliwa juu ya milima,[k] na-
nyi mtasikia sauti kama wa-
kati baragumu inapopigwa.[l]
4 Kwa maana Yehova amenia-
mbia hivi: "Nitakaa bila usu-
mbufu na kupatazama maha-
li pangu palipofanywa imara,[m]
kama joto linalometameta pa-
moja na nuru,[a] kama wingu la
umande katika joto la mavu-
no.[b] **5** Kwa maana kabla ya
mavuno, wakati ua linapofi-
kia ukamilifu na ua linapoku-
wa zabibu inayoiva, lazima mtu
pia akate vitawi kwa miundu
na kuviondoa vikonyo, lazima
avikate.[c] **6** Wote pamoja wa-
taachiwa ndege mwenye kuwi-
nda wa milimani na mnyama
wa dunia.[d] Na juu yao ndege
mwenye kuwinda atakaa waka-
ti wa kiangazi, na juu yao kila
mnyama wa dunia atakaa wa-
kati wa mavuno.[e]
7 "Katika wakati huo zawa-
di italetwa kwa Yehova wa ma-
jeshi,[f] kutoka kwa watu ware-
fu na walio laini,[g] kutoka kwa
watu wenye kuogopesha kila
mahali, taifa lenye nguvu zina-
zodumu na lenye kukanyaga-
kanyaga, ambalo mito imeifa-
gilia mbali nchi yake, kwenye
mahali pa jina la Yehova wa ma-
jeshi, Mlima Sayuni."[h]

19 Tangazo juu ya Misri:[i]
Tazama! Yehova amepa-
nda juu ya wingu jepesi[j] na ana-
kuja kuingia Misri. Na miungu
ya Misri isiyo na thamani ha-
kika itatetemeka kwa sababu
yake,[k] na moyo wa Misri utaye-
yuka katikati yake.[l]
2 "Nami nitawachochea Wa-
misri juu ya Wamisri, nao ha-
kika watapigana kila mmoja
na ndugu yake, na kila mmo-
ja na mwenzake, jiji juu ya jiji,
ufalme juu ya ufalme.[m] **3** Na
roho ya Misri lazima itatani-
shwe katikati yake,[n] nami nita-
vuruga shauri lake.[o] Nao haki-
ka wataenda kwa miungu isiyo
na thamani[p] na kwa wachawi

SURA 17
a Zb 29:3 Zb 65:7 Ufu 16:3 Ufu 17:1
b Zb 2:1 Zb 67:4 Isa 13:4
c Zb 9:5 Isa 33:3
d Zb 35:5 Zb 83:13 Isa 29:5 Da 2:35 Ho 13:3
e 2Fa 19:35 Zb 37:36
f Met 22:23 Isa 33:1 Eze 39:10 Sef 2:9

SURA 18
g Isa 20:3 Eze 30:4 Sef 3:10
h Isa 30:4 Eze 30:9
i 2Nya 12:3 2Nya 14:9 2Nya 16:8
j Zb 33:8 Zb 96:13 Met 8:31 Isa 26:18 Omb 4:12
k Isa 5:26 Isa 13:2
l Yoe 2:1 Amo 3:6 Zek 9:14
m Zb 132:13 Ho 5:15

Safu ya 2
a 2Sa 23:4
b Met 25:13
c Isa 5:7 Isa 17:11 Lu 8:14
d Isa 14:19 Eze 29:5
e Isa 34:3 Yer 15:3 Eze 32:4 Ufu 19:17
f 2Nya 32:23 Isa 2:2 Mal 1:11
g Isa 60:4 Zek 14:16
h Isa 8:18 Isa 24:23 Yoe 3:17 Mik 4:13

SURA 19
i Yer 25:19 Eze 29:2 Yoe 3:19
j Kum 33:26 Zb 68:33
k Kut 12:12 Yer 43:12 Yer 46:25 Eze 30:13
l Zb 76:12
m Mt 12:25
n Kum 7:20; Yos 2:11; o Met 19:21; Met 21:30; Isa 19:11; 1Ko 3:20; p Yer 16:20; 1Ko 8:4.

na kwa wenye kuwasiliana na pepo na kwa wajuzi wa kubashiri matukio.[a] **4** Nami nitaitia Misri katika mkono wa bwana mgumu, na mfalme atakayetawala juu yao atakuwa mwenye nguvu,"[b] asema Bwana wa kweli, Yehova wa majeshi.

5 Na maji hakika yatakauka kutoka baharini, na mto utakuwa mkavu na kwa kweli utakauka.[c] **6** Na lazima mito itoe harufu mbaya; mifereji ya Nile ya Misri lazima ishuke na kukauka.[d] Matete[e] na vitete lazima vioze. **7** Mahali palipo wazi kando ya Mto Nile, penye kinywa cha Mto Nile, na kila udongo wa kupanda mbegu wa Mto Nile zitakauka.[f] Hakika zitafukuziwa mbali, nazo hazitakuwapo tena. **8** Na wavuvi watalazimika kuomboleza, na wale wote wanaotupa ndoano ndani ya Mto Nile lazima wahuzunike, na hata wale wanaotandaza nyavu za kuvulia juu ya uso wa maji kwa kweli watadhoofika.[g] **9** Na wafanyakazi wa kitani[h] kilichochambuliwa lazima waone aibu; pia wafumaji wa nguo wa vitambaa vyeupe. **10** Na wafumaji[i] wake lazima wapondwe, wafanyakazi wote wa kulipwa wawe na huzuni katika nafsi.

11 Wakuu wa Soani[j] ni wapumbavu kwelikweli. Na kwa habari ya wenye hekima wa washauri wa Farao, shauri lao ni kitu kisicho cha akili.[k] Ninyi mtamwambiaje Farao: "Mimi ni mwana wa wenye hekima, mwana wa wafalme wa kale"? **12** Basi, wao wako wapi—watu wenu wenye hekima[l]—ili sasa wawaambie ninyi na ili wajue yale ambayo Yehova wa majeshi ameshauri kuhusu Misri?[a] **13** Wakuu wa Soani wametenda kwa upumbavu,[b] wakuu wa Nofu[c] wamedanganywa, wakuu wa makabila[d] yake wamesababisha Misri iende huku na huku. **14** Yehova mwenyewe amechanganya katikati yake roho ya mvurugo;[e] nao wamesababisha Misri kwenda huku na huku katika kazi yake yote, kama mtu aliyelewa anavyogaagaa katika matapiko yake.[f] **15** Na Misri haitakuwa na kazi yoyote ambayo inaweza kufanywa na kichwa wala mkia, chipukizi wala tete.[g]

16 Katika siku hiyo Misri itakuwa kama wanawake, nayo hakika itatetemeka[h] na kuingiwa na hofu kwa sababu ya kutikiswa kwa mkono wa Yehova wa majeshi ambao anautikisa juu yake.[i] **17** Na nchi ya Yuda itakuwa kisababishi cha kuyumba-yumba kwa Misri.[j] Kila mtu anayeambiwa juu yake ameingiwa na hofu kwa sababu ya shauri la Yehova wa majeshi ambalo anashauri juu yake.[k]

18 Katika siku hiyo kutakuwa na majiji matano katika nchi ya Misri[l] yanayosema lugha ya Kanaani[m] na kuapa[n] kwa Yehova wa majeshi. Jiji moja litaitwa Jiji la Kubomoa.

19 Katika siku hiyo kutakuwa na madhabahu kwa Yehova katikati ya nchi ya Misri,[o] na nguzo kwa Yehova kando ya mpaka wake. **20** Nayo itakuwa ni ishara na ushahidi kwa Yehova wa majeshi katika nchi ya Misri;[p] kwa maana watamlilia Yehova kwa sababu ya wakandamizaji,[q] naye atawapelekea mwokozi, aliye mkuu, ambaye kwa kweli atawakomboa.[r]

SURA 19

a Isa 8:19
Isa 44:25
Mdo 16:16
Ufu 18:23
b Yer 46:2
Yer 46:26
Eze 29:19
c Eze 30:12
Zek 10:11
d 2Fa 19:24
Isa 37:25
e Kut 2:3
Ayu 40:21
f Kum 11:10
Eze 29:10
g Hes 11:5
h Kut 9:31
Met 7:16
i Kut 35:35
j Hes 13:22
Zb 78:12
Isa 30:4
Eze 30:14
k Isa 44:25
1Ko 3:19
l Mwa 41:8
1Fa 4:30
Mhu 7:23
Mdo 7:22

Safu ya 2

a Ayu 11:7
Ro 11:33
b Ro 1:22
c Yer 46:14
Eze 30:13
Ho 9:6
d Amu 20:2
1Sa 14:38
e Ayu 12:20
Ayu 12:24
Isa 19:3
2Th 2:11
f Zb 107:27
Met 20:1
Isa 28:7
Yer 48:26
g Isa 9:15
h Zb 48:6
Yer 30:6
i Isa 10:32
Isa 11:15
Zek 2:9
j Yer 25:26
Yer 43:11
Eze 29:6
k Isa 14:24
Isa 20:3
Da 4:35
l Yer 43:7
Yer 44:1
Eze 30:14
m 2Fa 18:28
n Kum 10:20
Yer 4:2
Yer 12:16
o Yer 43:7
Yoh 17:15
Ufu 11:8
p Yer 32:20
q Zb 50:15
r Lu 2:11

21 Na Yehova hakika atajulikana kwa Wamisri;[a] na Wamisri lazima wamjue Yehova katika siku hiyo, nao watatoa dhabihu na zawadi[b] nao watamwekea Yehova nadhiri na kuitimiza.[c] **22** Na Yehova hakika ataipiga Misri.[d] Kutakuwako kupigwa na kuponywa;[e] nao lazima warudi kwa Yehova,[f] naye atakubali kusihi kwao na kuwaponya.[g]

23 Katika siku hiyo kutakuwa na njia kuu[h] kutoka Misri kwenda Ashuru, na Ashuru kwa kweli watakuja kuingia Misri, na Misri kuingia Ashuru; nao hakika watatoa utumishi, Misri pamoja na Ashuru. **24** Katika siku hiyo Israeli atakuwa wa tatu pamoja na Misri na pamoja na Ashuru,[i] yaani, baraka katikati ya dunia,[j] **25** kwa sababu Yehova wa majeshi atakuwa amewabariki,[k] akisema: "Wabarikiwe watu wangu, Misri, na kazi ya mikono yangu, Ashuru,[l] na urithi wangu, Israeli."[m]

20 Katika mwaka ule ambao Tartani[n] alikuja Ashdodi,[o] wakati Sargoni mfalme wa Ashuru alipomtuma,[p] naye akapigana vita na Ashdodi na kuliteka;[q] **2** wakati huo Yehova alisema kwa mkono wa Isaya mwana wa Amozi,[r] akisema: "Nenda,[s] ukavue nguo ya gunia kutoka viunoni mwako;[t] nawe uvue viatu vyako kutoka miguuni pako."[u] Naye akafanya hivyo, akitembea akiwa uchi na miguu wazi.[v]

3 Na Yehova akaendelea kusema: "Kama vile Isaya mtumishi wangu alivyotembea akiwa uchi na miguu wazi kwa miaka mitatu ili kuwa ishara[w] na dalili juu ya Misri[a] na juu ya Ethiopia,[b] **4** hivyo ndivyo mfalme wa Ashuru atakavyoliongoza kundi la mateka wa Misri[c] na wahamishwa wa Ethiopia, wavulana na wanaume wazee, wakiwa uchi na miguu wazi, na matako yakiwa wazi, uchi wa Misri.[d] **5** Nao hakika wataingiwa na woga na kuona aibu juu ya Ethiopia ambayo ni tumaini lao walilotazamia[e] na juu ya Misri ambayo ni uzuri wao.[f] **6** Na mkaaji wa nchi hii ya pwani atakuwa na hakika kusema siku hiyo, 'Tumaini letu tulilolitazamia liko hivyo, tulilokimbilia kupata msaada, ili kukombolewa kwa sababu ya mfalme wa Ashuru![g] Na sisi wenyewe tutaokoka jinsi gani?'"

21 Tangazo juu ya nyika ya bahari:[h] Kama kusonga mbele kwa pepo za dhoruba[i] upande wa kusini, jambo linakuja kutoka nyikani, kutoka katika nchi yenye kuogopesha.[j] **2** Kuna maono magumu[k] ambayo nimeambiwa: Mwenye kutenda kwa hila anatenda kwa hila, na mporaji anapora.[l] Nenda juu, Ee Elamu! Zingira, Ee Umedi![m] Nimekomesha kuugua kote kunakosababishwa naye.[n] **3** Ndiyo sababu viuno vyangu vimejaa maumivu makali.[o] Utungu umenishika, kama utungu wa mwanamke anayezaa.[p] Nimevurugika hivi kwamba sisikii; nimeingiwa na wasiwasi hivi kwamba sioni. **4** Moyo wangu umepigapiga; kutetemeka kumeniogopesha. Gizagiza la jioni ambalo

SURA 19
a Zb 83:18; Zb 98:2; Hab 2:14
b Sef 3:10; Mal 1:11
c Mhu 5:4
d Isa 19:1; Yer 46:13
e Kum 32:39; Isa 57:18; Yer 33:6; Ho 6:1
f Isa 19:18; Yer 44:1
g 1Fa 8:43; Yer 50:19; Zek 8:22
h Isa 11:16; Isa 35:8; Isa 40:3
i Kum 32:43; Zb 117:1; Zek 2:11
j Mwa 12:3; Eze 34:26; Zek 8:13; Ga 3:14
k Zb 67:6; Zb 115:12; Isa 61:9; Isa 65:8
l Ho 2:23; Ro 3:29
m Kum 32:9; Amo 3:2; Mal 3:17; 1Pe 2:9

SURA 20
n 2Fa 18:17
o Yos 11:22; Yos 13:3
p 2Nya 32:9
q Amo 1:8
r Isa 1:1
s Yer 13:1; Yer 19:1
t Yon 3:8; Ufu 11:3
u 2Sa 15:30
v 1Sa 19:24; Mik 1:8; Ebr 11:37
w Isa 8:18

Safu ya 2
a Isa 19:1
b Isa 18:1
c Isa 19:4; Yer 46:26; Eze 30:19
d Yer 13:22; Mik 1:11
e Zb 146:3
f 2Fa 18:21; Isa 30:3; Isa 36:6; Yer 17:5; Eze 29:6
g Isa 30:2; Isa 31:1

SURA 21 h Isa 13:1; Isa 13:20; Yer 51:42; i Zek 9:14; j Isa 13:4; Isa 13:18; k Isa 13:9; Ufu 18:2; l Isa 33:1; Yer 51:48; Yer 51:53; m Yer 51:11; Yer 51:28; Da 5:28; Da 8:20; n Zb 137:1; Isa 14:7; Isa 35:10; Yer 31:12; o Hab 3:16; p Yer 50:43; 1Th 5:3.

nililipenda limefanywa likawa kwangu kitu cha kutetemesha.[a]

5 Meza na ipangwe, viti vipangwe, kuwe na kula, kunywa![b] Simameni, enyi wakuu,[c] itieni ngao mafuta.[d] **6** Kwa maana Yehova ameniambia hivi:

“Nenda, weka mlinzi, ili aseme yale tu anayoyaona.”[e]

7 Naye akaona gari la vita pamoja na jozi ya farasi wa vita, gari la vita la punda, gari la vita la ngamia. Naye akasikiliza kwa makini, na kukaza fikira sana. **8** Naye akaita kama simba:[f] “Ee Yehova, juu ya mnara wa mlinzi ninasimama sikuzote wakati wa mchana, na kwenye kituo changu cha ulinzi ninasimama kila usiku.[g] **9** Na, tazama, sasa, linakuja gari la vita la watu, pamoja na jozi ya farasi wa vita!”[h]

Naye akaanza kusema: “Ameanguka! Babiloni ameanguka,[i] na sanamu zake zote za kuchongwa za miungu yake amezivunja na kuziangusha chini!”[j]

10 Enyi watu wangu waliopurwa na mwana wa uwanja wangu wa kupuria,[k] nimewaletea ninyi habari za yale ambayo nimeyasikia kutoka kwa Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli.

11 Tangazo juu ya Duma: Kuna mtu anayeniita kutoka Seiri:[l] “Mlinzi, kuna habari gani za usiku? Mlinzi, kuna habari gani za usiku?”[m] **12** Mlinzi akasema: “Lazima asubuhi ije, na usiku pia. Ikiwa ninyi mnataka kuuliza, ulizeni. Njooni tena!”

13 Tangazo juu ya nchi tambarare ya jangwani: Mtakaa usiku katika msitu katika nchi tambarare ya jangwani, enyi misafara ya watu wa Dedani.[a] **14** Leteni maji ili mkampokee mwenye kiu. Enyi wakaaji wa nchi ya Tema,[b] mpokeeni mtu anayekimbia mkiwa na mkate kwa ajili yake. **15** Kwa maana wamekimbia kwa sababu ya panga, kwa sababu ya upanga uliochomolewa, na kwa sababu ya upinde uliopindwa na kwa sababu ya ukali wa vita.

16 Kwa maana Yehova ameniambia hivi: “Katika muda wa mwaka mmoja, kulingana na miaka ya mfanyakazi wa kukodiwa,[c] utukufu wote wa Kedari[d] utafikia mwisho wake. **17** Na wale waliobaki kati ya hesabu ya wapiga-upinde, wale wanaume wenye nguvu wa wana wa Kedari, watakuwa wachache,[e] kwa maana Yehova mwenyewe, Mungu wa Israeli, amesema hivyo.”[f]

22 Tangazo la bonde la maono:[g] Una nini wewe, basi, hata nyote mkaenda juu ya paa?[h] **2** Ulijaa machafuko, jiji lenye msukosuko, mji wenye furaha.[i] Watu wako waliouawa hawakuuawa kwa upanga, wala hawakufa vitani.[j] **3** Madikteta[k] wako wote wamekimbia kwa wakati mmoja.[l] Wamechukuliwa kuwa wafungwa bila kuhitaji upinde. Watu wako wote ambao wamepatikana wamechukuliwa kuwa wafungwa pamoja.[m] Walikuwa wamekimbia kwenda mbali.

4 Ndiyo sababu nimesema: “Msinitazame. Nitaonyesha uchungu katika kulia.[n] Ninyi msisisitize juu ya kunifariji kwa sababu ya kuporwa kwa

SURA 21

a Kum 28:67
b Isa 22:13
Da 5:1
c Yer 50:35
Yer 51:57
d 2Sa 1:21
e 2Fa 9:17
Isa 62:6
Yer 51:12
Eze 3:17
Eze 33:3
Hab 2:1
Mt 24:45
f Isa 5:29
g Hab 2:1
h Yer 50:3
Yer 50:9
Yer 51:27
i Isa 13:19
Isa 14:4
Isa 45:1
Yer 50:3
Yer 51:8
Da 5:28
Ufu 14:8
Ufu 18:2
j Yer 50:2
Yer 51:44
Yer 51:52
k 1Fa 8:46
2Fa 13:7
Isa 1:25
Mt 3:12
Ebr 12:6
l Mwa 32:3
Kum 2:8
Zb 137:7
m Ufu 16:15

Safu ya 2

a Eze 27:15
b Ayu 6:19
Yer 25:23
c Ayu 7:1
Isa 16:14
d Mwa 25:13
Zb 120:5
Wim 1:5
Isa 42:11
Eze 27:21
e Yer 49:28
f Hes 23:19
Isa 46:10
Isa 55:11

SURA 22

g Isa 1:1
Isa 13:1
Isa 22:5
Yer 6:6
h Isa 15:3
Yer 48:38
i Isa 32:13
Amo 6:6
j Isa 3:1
Yer 14:18
Yer 38:2
Omb 4:9
k Isa 1:10
l 2Fa 25:4
Yer 39:4
Yer 52:7
m Yer 52:24
n Isa 33:7
Yer 4:19
Yer 6:26
Yer 9:1
Mik 1:8

binti ya watu wangu.[a] **5** Kwa
maana ni siku ya kuvurugika[b] na ya kukanyagiwa[c] chini na ya kufadhaisha[d] ambayo
Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi, anayo katika
bonde la maono. Kuna mbomoaji wa ukuta,[e] na kilio kitaenda
kwenye mlima.[f] **6** Na Elamu[g]
imelichukua podo, katika gari
la vita la mtu wa udongo, pamoja na farasi wa vita; na Kiri[h]
imeifunua ngao. **7** Na itatukia kwamba nchi zako tambarare za chini zilizo bora zaidi
zitajaa magari ya vita, na farasi wa vita lazima wajiweke katika lango, **8** na mtu atakiondoa kisitiri cha Yuda. Na siku
hiyo utatazama kulielekea ghala la silaha[i] la nyumba ya msitu,[j] **9** nanyi hakika mtayaona yale matundu ya ukuta wa
Jiji la Daudi, kwa maana kwa
kweli yatakuwa mengi.[k] Nanyi mtayakusanya maji ya kidimbwi cha chini.[l] **10** Nanyi
kwa kweli mtazihesabu nyumba za Yerusalemu. Nanyi pia
mtazibomoa nyumba ili kuufanya ukuta[m] usiweze kufikiwa.
11 Nanyi lazima mfanye beseni kati ya hizo kuta mbili kwa
ajili ya kukusanya maji ya kidimbwi cha kale.[n] Nanyi hakika
hamtamtazama Mtengenezaji Mkuu wake, na yeye aliyeifanya zamani za kale hakika
hamtamwona.

12 "Na Bwana Mwenye Enzi
Kuu,[o] Yehova wa majeshi, atataka katika siku hiyo kuwe kilio[p]
na maombolezo na upara
na kuvaa nguo za magunia.[q]
13 Lakini, tazama! furaha na
shangwe, kuchinja ng'ombe
na kuchinja kondoo, kula nyama na kunywa divai,[r] 'Na tule
na tunywe, kwa maana kesho
tutakufa.'"[a]

14 Na Yehova wa majeshi
amejifunua masikioni mwangu:[b] "'Kosa hili halitafanyiwa upatanisho[c] kwa ajili yenu
mpaka mtakapokufa,'[d] Bwana
Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa
majeshi, amesema."

15 Bwana Mwenye Enzi
Kuu, Yehova wa majeshi, amesema hivi: "Nenda, ingia kwa
huyu msimamizi-nyumba, kwa
Shebna,[e] aliye juu ya nyumba,[f]
16 'Hapa kuna nini ambacho
ni haki yako, na hapa kuna
nani ambaye ni haki yako, hata
ukajichimbia hapa kaburi?'[g]
Anachimba kaburi lake juu
ya kilele; anajichongea makao katika mwamba. **17** 'Tazama! Yehova anakutupa chini
kwa mtupo wenye jeuri,
Ee mwanamume, na kukushika kwa nguvu. **18** Bila shaka atakufunga imara, kama
mpira kwa ajili ya nchi pana.
Utakufa huko, na huko magari ya utukufu wako yatakuwa aibu ya nyumba ya bwana wako. **19** Nami nitakusukuma utoke katika cheo chako; na mtu atakuondoa katika
cheo chako rasmi.[h]

20 "'Na lazima itatukia katika siku hiyo kwamba nitamwita mtumishi wangu,[i] yaani, Eliakimu[j] mwana wa Hilkia.[k]
21 Nami nitamvika kanzu
yako, nitamfunga imara ukumbuu wako,[l] nitaitia mkononi mwake mamlaka yako; naye
lazima awe baba kwa mkaaji
wa Yerusalemu na kwa nyumba ya Yuda.[m] **22** Nami nitauweka ufunguo[n] wa nyumba ya
Daudi juu ya bega lake, naye
atafungua bila mtu yeyote

SURA 22

a Yer 8:18
Yer 31:15
b Yer 30:5
Amo 5:18
c Isa 5:5
Isa 10:6
d Mik 7:4
e 2Fa 25:10
Ne 1:3
Omb 2:2
f Ho 10:8
Lu 23:30
Ufu 6:16
g Mwa 10:22
Isa 21:2
h 2Fa 16:9
Amo 1:5
i Ne 3:19
j 1Fa 7:2
k 2Fa 25:10
Yer 52:7
l 2Fa 20:20
2Nya 32:30
Ne 3:15
Yoh 9:7
m Ne 1:3
n 2Fa 18:17
Isa 7:3
Isa 36:2
o Mdo 4:24
p Ne 8:9
Isa 15:3
Yoe 2:17
q Ayu 1:20
Amo 8:10
Mik 1:16
r Isa 5:12
Isa 56:12
Amo 6:4
Lu 17:27

Safu ya 2

a Isa 21:5
1Ko 15:32
Yak 5:5
b Isa 5:9
Amo 3:7
c Isa 1:11
Yer 15:1
Eze 24:13
Ebr 10:26
d Law 26:31
e 2Fa 18:37
2Fa 19:2
Isa 36:3
Isa 37:2
f 2Fa 10:5
g Isa 14:18
Mt 27:60
h Ayu 40:11
Zb 75:7
Lu 1:52
i Mt 24:45
1Ko 4:2
j 2Fa 18:18
2Fa 18:37
Isa 36:3
k 2Fa 18:26
l Mwa 41:42
1Sa 18:4
Est 8:15
m Mwa 45:8
n 1Nya 9:27
Ufu 3:7

kufunga, atafunga bila mtu yeyote kufungua.[a] **23** Nami nitampigilia kama kigingi[b] mahali panapodumu, naye lazima awe kama kiti cha ufalme cha utukufu kwa nyumba ya baba yake.[c] **24** Nao wataning'iniza juu yake utukufu wote wa nyumba ya baba yake, wazao na machipukizi, vyombo vyote vya aina ndogo, vyombo vya aina ya bakuli na vilevile vyombo vya mitungi mikubwa.

25 "'Katika siku hiyo,' asema Yehova wa majeshi, 'kile kigingi[d] ambacho kimepigiliwa mahali panapodumu kitang'olewa,[e] nacho kitakatwa na kuanguka, na mzigo ulio juu yake utakatiliwa mbali, kwa maana Yehova mwenyewe amesema hayo.'"[f]

23 Tangazo la Tiro:[g] Pigeni mayowe, enyi meli za Tarshishi![h] kwa maana imeporwa isiwe bandari tena, isiwe mahali pa kuingia.[i] Wamefunuliwa habari kutoka katika nchi ya Kitimu.[j] **2** Kaeni kimya, enyi wakaaji wa nchi ya pwani. Wanabiashara kutoka Sidoni,[k] wale wanaovuka bahari—wamekujaza. **3** Na mbegu ya Shihori[l] imekuwa juu ya maji mengi, mavuno ya Nile, mapato yake; nayo yakaja kuwa faida ya mataifa.[m]

4 Ona aibu, Ee Sidoni;[n] Ee ngome ya bahari, kwa sababu bahari imesema: "Sijapata uchungu wa kuzaa, nami sijazaa, wala sijalea vijana, wala kulea mabikira."[o] **5** Kama vile wakati wa ile habari juu ya Misri,[p] ndivyo watu watakavyokuwa na maumivu makali wakati wa ile habari juu ya Tiro.[q]

SURA 22

a Mt 18:18
b Ezr 9:8
c Mwa 45:9
1Sa 2:8
Lu 22:30
Ufu 3:21
d Isa 22:15
e Isa 22:17
f Isa 46:11
Yer 4:28

SURA 23

g Yer 25:22
Yer 47:4
Eze 26:3
Eze 27:2
Yoe 3:4
Amo 1:9
Zek 9:4
h 2Nya 9:21
Zb 48:7
Isa 2:16
Eze 27:25
i Eze 27:3
j Mwa 10:4
Yer 2:10
Eze 27:6
Da 11:30
k Eze 27:8
l Yer 2:18
m Eze 27:33
Eze 28:4
Yoe 3:5
n Mwa 10:15
Eze 27:8
o Yer 47:4
p Isa 19:1
Isa 19:16
q Eze 26:15
Eze 27:35
Eze 28:19

Safu ya 2

a Kum 29:24
Zb 94:2
b Eze 28:2
c Isa 14:24
Isa 46:10
d Da 4:37
Yak 4:6
e Ayu 12:21
Zb 107:40
f Isa 23:1
g Eze 26:14
Eze 26:17
h Zb 46:6
Eze 27:34
i Eze 26:5
Eze 26:15
j Eze 26:13
k Mwa 10:15
l Eze 27:6
Da 11:30
m Mwa 11:31
Isa 13:19
Isa 47:1
Hab 1:6
n 2Fa 17:24
Isa 10:12
Isa 30:31
Nah 3:18
Sef 2:13
o Isa 13:21
p Eze 26:8
q Eze 26:9
r Eze 26:12
s Isa 23:1

6 Vukeni mpaka Tarshishi; pigeni mayowe, enyi wakaaji wa nchi ya pwani. **7** Je, hili ndilo jiji lenu lililokuwa na furaha tangu siku za kale, tangu nyakati zake za zamani? Miguu yake ilikuwa ikimpeleka mbali kukaa kama mgeni.

8 Ni nani ambaye ametoa shauri hili[a] juu ya Tiro, mwenye kuvika watu mataji, ambaye wanabiashara wake walikuwa wakuu, ambaye wafanyabiashara wake walikuwa watu wenye vyeo wa dunia?[b]

9 Yehova wa majeshi mwenyewe ametoa shauri hili,[c] kutia unajisi kiburi cha uzuri wote,[d] kuwatendea kwa dharau watu wote wenye vyeo wa dunia.[e]

10 Vuka juu ya nchi yako kama Mto Nile, Ee binti Tarshishi.[f] Hakuna tena kiwanda cha meli.[g] **11** Ameunyoosha mkono wake juu ya bahari; amezifadhaisha falme.[h] Yehova mwenyewe ametoa amri juu ya Foinike, ya kuziangamiza ngome zake.[i] **12** Naye asema: "Usifurahi kamwe tena,[j] ewe uliyekandamizwa, bikira binti Sidoni.[k] Simama, vuka mpaka Kitimu.[l] Hata huko hakutakuwa na utulivu kwako."

13 Tazama! Nchi ya Wakaldayo.[m] Hiki ndicho kikundi cha watu—Ashuru[n] hakujionyesha kuwa hicho—walimweka awe msingi kwa ajili ya wakaaji wa jangwani.[o] Wamesimamisha minara yao ya kuzingira;[p] wameivua minara yake ya makao;[q] mtu amemweka kuwa bomoko linaloharibika.[r]

14 Pigeni mayowe, enyi meli za Tarshishi, kwa maana ngome yenu imeporwa.[s]

15 Na itatukia katika siku hiyo kwamba Tiro lazima lisahauliwe kwa miaka 70,[a] sawasawa na siku za mfalme mmoja. Mwishoni mwa ile miaka 70 itakuwa kwa Tiro kama katika wimbo wa kahaba: **16** "Chukua kinubi, lizunguke jiji, Ee kahaba uliyesahauliwa.[b] Fanya kila unaloweza kupiga vinanda; fanya nyimbo zako ziwe nyingi, ili upate kukumbukwa."

17 Na itatukia kwamba mwishoni mwa miaka 70 Yehova atakaza fikira zake juu ya Tiro, naye atarudia malipo[c] yake na kufanya ukahaba na falme zote za dunia zilizo juu ya uso wa nchi.[d] **18** Na faida yake na malipo[e] yake lazima viwe kitu kitakatifu kwa Yehova. Havitawekwa akiba, wala kurundikwa, kwa sababu malipo yake yatakuja kuwa ya wale wanaokaa mbele za Yehova,[f] kwa ajili ya kula na kushiba na kwa ajili ya mavazi yenye fahari.[g]

24 Tazama! Yehova anaifanya nchi kuwa tupu na kuifanya ukiwa,[h] naye amepotoa uso wake[i] na kuwatawanya wakaaji wake.[j] **2** Na itakuwa kwa watu kama vile ilivyo kwa kuhani; itakuwa kwa mtumishi kama vile ilivyo kwa bwana wake; itakuwa kwa mjakazi kama vile ilivyo kwa bimkubwa wake; itakuwa kwa mnunuzi kama vile ilivyo kwa muuzaji; itakuwa kwa mkopeshaji kama vile ilivyo kwa mkopaji; itakuwa kwa mchukua-faida kama vile ilivyo kwa mlipa-faida.[k] **3** Hakika nchi itafanywa kuwa tupu, na hakika itaporwa,[l] kwa maana Yehova mwenyewe amesema neno hilo.[a] **4** Nchi imeomboleza,[b] imefifia. Nchi yenye kuzaa imenyauka, imefifia. Wakuu wa watu wa nchi wamenyauka.[c] **5** Nayo nchi imechafuliwa chini ya wakaaji wake,[d] kwa maana wamezivunja sheria,[e] wamelibadili sharti,[f] wamevunja agano linalodumu mpaka wakati usio na kipimo.[g] **6** Ndiyo sababu laana imeila nchi,[h] na wakaaji wake wamehesabiwa hatia. Ndiyo sababu wakaaji wa nchi wamepungua hesabu, na wanadamu wanaoweza kufa walio wachache sana ndio wamebaki.[i]

7 Divai mpya imeomboleza, mzabibu umenyauka,[j] wote wenye furaha moyoni wameanza kuugua.[k] **8** Furaha ya matari imekoma, kelele za waliosimuka sana zimekoma, furaha ya kinubi imekoma.[l] **9** Wanakunywa divai bila wimbo wowote; kileo kinakuwa kichungu kwa wale wanaokinywa. **10** Mji uliohamwa umebomolewa;[m] kila nyumba imefungwa isiingiwe. **11** Kuna kilio barabarani kwa sababu ya upungufu wa divai. Shangwe yote imepitilia mbali; furaha ya nchi imeondoka.[n] **12** Hali ya kushangaza imeachwa nyuma katika jiji; lango limebomolewa na kuwa tuta tupu la mabomoko.[o]

13 Kwa maana itakuwa hivyo katikati ya nchi, katikati ya vikundi vya watu, kama kupigwa kwa mzeituni,[p] kama masalio wakati ukusanyaji wa zabibu umemalizika.[q] **14** Wao

SURA 23
a Yer 25:11; Yer 27:3; Yer 27:6
b Met 7:10; Yer 30:14
c Mik 1:7
d Nah 3:4
e Kum 23:18
f Ayu 27:17; Mhu 2:26
g Isa 60:5; Isa 61:6

SURA 24
h Kum 28:63; Isa 1:7; Isa 5:5; Yer 4:6; Eze 6:6
i 2Fa 21:13
j Kum 28:64; Ne 1:8; Yer 9:16
k Isa 3:2; Isa 9:14; Eze 7:12; Ho 4:9
l Law 26:31; Kum 29:28

Safu ya 2
a Isa 46:10
b Isa 3:26; Isa 33:9; Yer 4:28; Omb 1:4; Ho 4:3
c Isa 2:11
d Law 18:24; Hes 35:33; 2Nya 33:9; Yer 3:1; Yer 23:11; Omb 4:13
e 2Fa 17:7; 2Fa 22:13; Eze 20:13; Da 9:5
f Mik 3:11
g Kut 19:5; Kut 24:7; Yer 31:32; Yer 34:18
h Law 26:16; Kum 28:15; Yos 23:15
i Law 26:22; Kum 4:27; Kum 28:62; Isa 10:22
j Yer 8:13; Yoe 1:10
k Isa 16:10; Isa 32:12; Amo 5:17
l Zb 81:2; Yer 7:34; Yer 16:9; Ho 2:11
m 2Fa 25:10
n Isa 8:22; Omb 5:15
o Isa 32:14; Yer 9:11; Omb 1:4; Omb 2:9; Mik 1:9
p Kum 24:20; Isa 17:6
q Isa 1:9; Isa 17:5; Yer 6:9; Eze 6:8; Mik 7:1.

wenyewe watapaaza sauti yao,
watapiga vigelegele kwa shangwe. Hakika watapaaza vilio vya shangwe kutoka baharini kwa ukuu wa Yehova.[a]
15 Ndiyo sababu katika eneo
la nuru[b] watamtukuza Yehova,[c]
katika visiwa vya bahari jina
la Yehova,[d] Mungu wa Israeli.
16 Kuna muziki ambao tumesikia kutoka mwisho wa nchi:[e]
"Pambo kwake Aliye Mwadilifu!"[f]

Lakini nasema: "Mimi nimekonda,[g] mimi nimekonda! Ole wangu! Wanaotenda hila wametenda kwa hila.[h] Wanaotenda hila wametenda kwa hila."[i]

17 Hofu na shimo na mtego ziko juu yako, wewe mkaaji wa nchi.[j] **18** Na itatukia
kwamba yeyote anayeikimbia
sauti ya kitu kinachotia hofu
ataanguka katika shimo, na yeyote anayetoka ndani ya shimo
atakamatwa katika mtego.[k] Kwa maana milango ya
maji ambayo iko juu itafunguliwa,[l] na misingi ya nchi itatikisika.[m] **19** Nchi imepasuka
kabisa, nchi imetikiswa kabisa,
nchi imeyumbishwa-yumbishwa kabisa.[n] **20** Nchi inasonga
kwa kuyumba-yumba
kabisa kama mlevi, nayo imeyumba huku na huku kama
kijumba cha mlinzi.[o] Na makosa yake yamekuwa mazito juu yake,[p] nayo itaanguka, hivi kwamba haitasimama tena.[q]

21 Na itatukia katika siku
hiyo kwamba Yehova ataelekeza fikira zake juu ya jeshi lililo juu mahali pa juu, na juu ya
wafalme wa nchi juu ya nchi.[r]
22 Nao hakika watakusanywa
kama kukusanywa kwa wafungwa ndani ya shimo,[s] na kufungiwa ndani ya gereza la shimoni;[a] na baada ya siku nyingi
watakaziwa fikira.[b] **23** Na
mwezi mpevu umefedheheka,
na jua linaloangaza limeona
aibu,[c] kwa maana Yehova wa
majeshi amekuwa mfalme[d] katika Mlima Sayuni[e] na katika Yerusalemu na mbele ya wanaume wake wazee kwa utukufu.[f]

25 Ee Yehova, wewe ni Mungu wangu.[g] Ninakutukuza,[h] ninalisifu jina lako,[i] kwa
maana umetenda mambo ya
ajabu,[j] mashauri[k] kutoka nyakati za kale, kwa uaminifu,[l]
kwa kutegemeka.[m] **2** Kwa
maana umefanya jiji kuwa fungu la mawe, mji wenye ngome kuwa bomoko linaloanguka, mnara wa makao ya wageni usiwe jiji, ambalo halitajengwa upya mpaka wakati usio na kipimo.[n] **3** Ndiyo sababu wale ambao ni kikundi
cha watu wenye nguvu watakutukuza wewe; mji wa mataifa yenye kuonea, watakuogopa.[o] **4** Kwa maana umekuwa
ngome kwa mtu wa hali ya chini, ngome kwa maskini katika taabu aliyo nayo,[p] kimbilio kutokana na dhoruba ya mvua,
kivuli[q] kutokana na joto, wakati mlipuko wa wenye kuonea
ni kama dhoruba ya mvua juu
ya ukuta. **5** Kama joto katika nchi isiyo na maji, unazitiisha kelele za wageni, joto kwa
kivuli cha wingu.[r] Muziki wa watu wenye kuonea unanyamazishwa.[s]

6 Na Yehova wa majeshi ha-

SURA 24
a Isa 12:1; Isa 40:9; Yer 31:12; Yer 33:11; Zek 2:10
b Kut 27:13; Zb 97:11; Isa 30:26; Isa 43:5; Isa 49:6; Mik 7:9
c Zek 13:9; Mal 1:11
d Isa 11:11; Isa 60:9; Sef 2:11
e Zb 22:27; Zb 98:3; Mk 13:27
f Kut 15:11; Ezr 9:15; Zb 145:7; Ufu 15:3; Ufu 19:2
g Isa 10:16; Isa 17:4
h Isa 21:2; Isa 33:1; Omb 1:2
i Yer 9:2; Ho 10:13
j Law 26:22; Yer 8:3; Eze 14:21; Amo 5:19
k Kum 32:23; 1Fa 20:30
l Mwa 7:11; Met 27:4
m Kum 32:22; Zb 18:7; Zb 18:15
n Yer 4:24; Nah 1:5; Hab 3:6
o Zb 107:27; Isa 19:14; Isa 29:9
p 2Fa 21:16; 2Nya 36:16; Yer 14:20; Ho 4:2
q Amo 8:14
r Zb 76:12; Hag 2:22
s Mwa 41:14

Safu ya 2
a Isa 42:7
b Zek 9:11
c Ufu 21:23
d Zb 97:1; Ufu 11:17
e Zb 132:13; Isa 8:18; Isa 18:7; Yoe 3:17; Ebr 12:22
f 1Fa 8:11; Zb 46:5; Isa 12:6; Mik 4:7; Zek 2:10

SURA 25
g Kum 32:3; 1Nya 29:10; Zb 25:12; Isa 61:10
h Zb 7:17; Zb 99:5; Zb 145:1; Ebr 13:15
i Zb 30:4; Zb 150:6; Ufu 15:4;
j Zb 40:5; Zb 98:1; Zb 107:8; Zb 145:4;
k Zb 33:11; Isa 28:29; Ebr 6:17;
l Kum 32:4; Ne 9:33; Zb 89:5;
m Mwa 24:27; Hes 23:19;
n Kum 13:16; Isa 6:11;
o Zb 46:10; Zb 66:3; Zb 83:16; Eze 38:23;
p Zb 46:1; Zb 121:7; Nah 1:7; Sef 3:12;
q Zb 91:1; Zb 121:5; Zb 121:6; Ufu 7:16;
r Ayu 7:2; Isa 49:10;
s Zb 58:10; Isa 24:8; Ufu 18:22.

kika atavifanyia vikundi vyote
vya watu,[a] katika mlima huu,[b]
karamu ya vyakula vinono vili-
vyotiwa mafuta,[c] karamu ya di-
vai iliyowekwa kwenye machi-
cha, ya vyakula vinono vilivyo-
tiwa mafuta vilivyojazwa uro-
jorojo,[d] ya divai[e] iliyowekwa
kwenye machicha, iliyochu-
jwa.[f] **7** Na katika mlima huu
hakika ataumeza uso wa kifu-
niko kinachovifunika vikundi
vyote vya watu,[g] na mfumo uli-
ofumwa kwa kusokotana juu
ya mataifa yote. **8** Yeye kwa
kweli atameza kifo milele,[h] na
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova hakika atafuta machozi
katika nyuso zote.[i] Na shutu-
ma ya watu wake ataiondoa ka-
tika dunia yote,[j] kwa maana
Yehova mwenyewe amesema
hayo.

9 Na katika siku hiyo ha-
kika mtu atasema: "Tazama!
Huyu ndiye Mungu wetu.[k] Tu-
memtumaini yeye,[l] naye ata-
tuokoa.[m] Huyu ndiye Yehova.[n]
Tumemtumaini yeye. Na tuwe
na shangwe na kushangilia ka-
tika wokovu wake."[o]

10 Kwa maana mkono wa
Yehova utatua juu ya mli-
ma huu,[p] na Moabu atakanya-
gwa chini[q] katika mahali pake
kama fungu la majani linavyo-
kanyagwa chini katika mahali
penye mbolea.[r] **11** Naye ata-
piga mikono yake katikati yake
kama mwogeleaji anavyoifa-
nya mikono yake, naye atashu-
sha majivuno[s] yake kwa mwe-
ndo wa udanganyifu wa mi-
kono yake. **12** Na lile jiji len-
ye ngome, pamoja na kuta
zako ndefu za usalama, ata-
lilaza chini; atalishusha, atali-
angusha chini kwenye dunia,
kwenye mavumbi.[t]

SURA 25

a Isa 49:10
Da 7:14
Mt 8:11
b Zb 72:3
Isa 11:9
Isa 65:25
Da 2:35
c Zb 72:16
Zb 85:11
Zb 85:12
Zb 104:15
Yer 31:12
d Ayu 21:24
e Mhu 10:19
Isa 55:1
f Yer 48:11
Lu 5:39
g Isa 60:2
Lu 2:32
Mdo 17:30
2Ko 3:13
2Ko 4:4
Efe 5:8
h Ho 13:14
1Ko 15:54
2Ti 1:10
Ebr 2:15
Ufu 20:14
i Isa 35:10
Ufu 7:17
Ufu 21:4
j Zb 69:9
Zb 89:51
k Kum 32:3
Isa 25:1
Ufu 19:1
l Zb 27:14
Zb 37:34
Zb 146:5
m Mwa 49:18
Met 20:22
Lu 2:30
n Kut 6:2
Zb 97:5
Sef 3:12
o Zb 20:5
Zb 21:1
Zb 62:1
Zb 95:1
Mik 7:7
Sef 3:14
p Zb 132:13
Isa 12:6
q Zb 110:6
Isa 15:1
Sef 2:9
r Zb 83:10
Lu 13:8
s Yer 48:29
Da 4:37
Yak 4:6
t Isa 26:5

Safu ya 2

SURA 26

a Isa 4:2
Isa 26:19
Yoh 11:24
b Kut 15:1
2Sa 22:1
Zb 146:2
Zb 150:5
Isa 12:5
c Yer 33:10
Yer 33:11
d Zb 48:2
Zb 48:12
Zb 127:1
e Isa 60:18
Zek 2:5

26 Katika siku hiyo[a] wimbo
huu utaimbwa[b] katika
nchi ya Yuda:[c] "Tuna jiji len-
ye nguvu.[d] Yeye anaweka wokovu
kuwa kuta na boma.[e] **2** Fu-
ngueni malango,[f] ili taifa la
uadilifu linaloshika mwenendo
wa uaminifu liingie.[g] **3** Mwe-
lekeo ambao umetegemezwa
vema utaulinda katika amani
ya kudumu,[h] kwa sababu huyo
hufanywa akutegemee wewe.[i]
4 Mtegemeeni Yehova,[j] kwa
nyakati zote, kwa maana kati-
ka Yah Yehova kuna Mwamba[k]
wa mpaka nyakati zisizo na ki-
pimo.

5 "Kwa maana amewashu-
sha chini wale wanaokaa juu
ya kilele,[l] mji ulioinuliwa.[m]
Yeye anaushusha, anaushusha
mpaka duniani; anauleta kwe-
nye mavumbi.[n] **6** Mguu utau-
kanyagia chini, miguu ya mwe-
nye kuteseka, nyayo za watu
wa hali ya chini."[o]

7 Pito la mwadilifu ni unyo-
ofu.[p] Kwa kuwa wewe ni mnyo-
ofu, utaifanya njia ya mwa-
dilifu kuwa laini.[q] **8** Ndiyo,
kwa ajili ya njia ya hukumu
zako, Ee Yehova, tumekutuma-
ini wewe.[r] Tamaa ya nafsi ime-
kuwa kwa ajili ya jina lako na
kwa ajili ya ukumbusho wako.[s]
9 Nimekutamani wewe kwa
nafsi yangu usiku;[t] ndiyo, nina-
endelea kukutafuta kwa roho
yangu ndani yangu;[u] kwa saba-
bu, wakati kunapokuwa na hu-
kumu kutoka kwako kwa ajili

f Zb 118:19; Zb 118:20; Isa 60:11; Isa 62:10; Mt 7:14; Ufu 22:14; g Kut 19:6; Kum 4:8; Mal 3:17; Mdo 2:47; 1Pe 2:9; h Zb 119:165; Isa 54:13; Yoh 14:27; Ro 15:33; Flp 4:7; 2Pe 1:2; i Zb 9:10; Yer 17:7; j 2Nya 20:20; Zb 62:8; Met 3:5; k Kum 32:4; Kum 32:31; 1Sa 2:2; l Ayu 40:11; Isa 2:11; m Isa 15:1; Isa 25:10; n Isa 25:12; Yer 48:9; o Sef 3:12; Mal 4:3; p 1Nya 29:17; Ayu 1:1; Zb 18:24; Met 20:7; q Zb 5:8; r Zb 119:7; Efe 5:17; s Kut 3:15; Zb 135:13; Ho 12:5; Mik 7:7; t Zb 63:6; Zb 119:62; Lu 6:12; u Zb 63:1; Zb 77:6.

ya dunia,[a] wakaaji wa nchi yenye kuzaa hakika watajifunza uadilifu.[b] **10** Hata mwovu akionyeshwa kibali, yeye hatajifunza uadilifu.[c] Atatenda isivyo haki katika nchi ya unyoofu,[d] naye hatauona ukuu wa Yehova.[e]

11 Ee Yehova, mkono wako umeinuliwa juu,[f] lakini wao hawauoni.[g] Wataona na kupata aibu[h] kutokana na bidii kwa ajili ya watu wako. Ndiyo, moto[i] kwa ajili ya adui zako utawateketeza wao. **12** Ee Yehova, utatuhukumia amani,[j] kwa sababu umetenda kazi zetu zote kwa ajili yetu.[k] **13** Ee Yehova Mungu wetu, mabwana wengine mbali na wewe wamekuwa wamiliki wetu.[l] Ni kwa msaada wako wewe peke yako tutalitaja jina lako.[m] **14** Wao wamekufa; hawataishi.[n] Wakiwa ni wasiojiweza katika kifo,[o] hawataamka.[p] Kwa hiyo umeelekeza fikira zako ili uwaangamize na kuharibu majina yao yote.[q]

15 Umeliongezea hilo taifa; Ee Yehova, umeliongezea hilo taifa;[r] umejitukuza mwenyewe.[s] Umeieneza mbali mipaka yote ya nchi hiyo.[t] **16** Ee Yehova, wakati wa taabu wamekuelekezea fikira zao;[u] wametoa mnong'ono wa sala walipopata nidhamu[v] yako. **17** Kama vile mwanamke mwenye mimba anapokaribia kuzaa, anavyopata maumivu, hulia akiwa katika maumivu yake ya kuzaa, ndivyo tumekuwa kwa sababu yako, Ee Yehova.[w] **18** Tumepata mimba, tumekuwa na maumivu ya kuzaa;[x] ni kana kwamba sisi tumezaa upepo. Hatutimizi wokovu wowote ulio halisi kuhusiana na nchi,[a] wala hakuna wakaaji wowote wa nchi yenye kuzaa wanaoanguka katika kuzaliwa.[b]

19 "Wafu wako wataishi.[c] Maiti wangu—wataamka.[d] Amkeni, pigeni vigelegele kwa shangwe, enyi mnaokaa mavumbini![e] Kwa maana umande[f] wako ni kama umande wa miholi,[g] na dunia itawaacha hata wale wasiojiweza katika kifo waanguke katika kuzaliwa.[h]

20 "Nendeni, watu wangu, ingia katika vyumba vyako vya ndani, na ufunge milango nyuma yako.[i] Jifiche kwa kitambo kidogo mpaka hukumu itakapopita.[j] **21** Kwa maana, tazama! Yehova anakuja kutoka mahali pake ili kulitoza hesabu kosa la mkaaji wa nchi juu yake,[k] na nchi hakika itafunua umwagaji wake wa damu[l] wala haitawafunika tena watu wake waliouawa."[m]

27 Katika siku ile Yehova,[n] akiwa na upanga wake mgumu na wenye nguvu,[o] atalekeza uangalifu wake juu ya Lewiathani,*[p] yule nyoka anayenyiririka,[q] juu ya Lewiathani, yule nyoka mpotovu, na hakika yeye atamuua huyo mnyama mkubwa wa baharini[r] aliye ndani ya bahari.

2 Katika siku ile mwimbieni huyo mwanamke:[s] "Shamba la mizabibu[t] la divai yenye kutoa povu! **3** Mimi, Yehova, ni-

SURA 26

a Zb 9:8; Zb 58:11
b Zb 85:11; Zb 96:13; Zb 97:2; Isa 61:11
c Kut 8:15; Zb 106:43; Met 1:32
d Zb 78:57; Yer 2:7
e Zb 28:5; Isa 5:12; Ho 11:7
f Zb 10:12; Mik 5:9
g Isa 6:9
h Zb 86:17; 1Pe 3:16; Ufu 3:9
i Ebr 10:27
j Zb 29:11; Isa 57:19; Yer 33:6; Yoh 14:27
k Mdo 5:38; Mdo 5:39
l 2Nya 12:8
m Yos 23:7; 2Ti 2:19
n Zb 22:15
o Met 2:18; Mhu 9:5; Mhu 9:10; Isa 38:18
p Ayu 14:14; Mhu 9:6; Yer 51:39; Mt 25:46
q Zb 9:5; Zb 109:13; Met 10:7
r Mwa 12:2; Kum 10:22; Isa 9:3; Isa 51:2
s Zb 72:18; Isa 60:21
t 1Fa 4:21
u Amu 10:10; Zb 77:2; Zb 78:34; Ho 5:15
v Amu 3:8; Ebr 12:5; Ebr 12:6
w Isa 13:8; Yer 4:31; Yer 6:24
x 2Fa 19:3

Safu ya 2

a Yos 7:9
b Isa 37:3
c Ho 13:14; Yoh 5:29; Mdo 24:15; 1Ko 15:22; Ufu 20:12
d Isa 25:8; Mk 12:26; Yoh 11:24; Yoh 11:25; 1Ko 15:21; 1Th 4:14
e Mwa 3:19; Da 12:2
f Eze 37:2
g 2Fa 4:39
h Ufu 20:13; i Mwa 7:16; Kut 12:22; Zb 32:7; Zb 91:4; Met 18:10; j Zb 27:5; Zb 57:1; Zb 91:4; k Zb 37:20; Ho 5:14; Mik 1:3; Mt 24:21; 2Th 1:8; 2Pe 3:7; l Mwa 4:10; Zb 9:12; Eze 24:7; Lu 11:50; Ufu 16:6; Ufu 18:24; m Mal 4:1; **SURA 27** n Kut 15:3; o Kum 32:41; Yer 47:6; p Ayu 41:1; q Ayu 26:13; r Mwa 1:21; Zb 74:13; Isa 51:9; Eze 29:3; Eze 32:2; s Isa 5:1; t Zb 80:8; Yer 2:21; Mt 21:33.

Isa 27:1* Pengine mamba.

namlinda yeye.[a] Nitamnywesha maji kila wakati.[b] Ili yeyote asielekeze fikira zake kupigana naye, nitamlinda usiku na mchana.[c] **4** Mimi sina ghadhabu.[d] Ni nani atakayenipa vichaka vya miiba[e] na magugu katika pigano? Nitavikanyaga hivyo. Nitaviwasha moto kwa wakati mmoja.[f] **5** Kama sivyo na ashike ngome yangu, na afanye amani pamoja nami; na afanye amani pamoja nami."[g]

6 Katika siku zinazokuja Yakobo atatia mizizi, Israeli[h] atachanua maua na kwa kweli achipuke; na kwelikweli wao watajaza matunda juu ya uso wa nchi yenye kuzaa.[i]

7 Je, ni lazima mtu ampige kwa pigo kama la mtu anayempiga? Au, je, ni lazima auawe kwa mauaji kama ya watu wake waliouawa?[j] **8** Utashindana naye kwa mlio wa kushtua utakapokuwa ukimfukuza. Lazima yeye atamfukuza huyo kwa mlipuko wake, ulio mkali katika siku ya upepo wa mashariki.[k] **9** Basi kwa njia hii kosa la Yakobo litafanyiwa upatanisho,[l] na haya ni matunda yote wakati anapoiondoa dhambi yake,[m] wakati anapofanya mawe yote ya madhabahu kama mawe ya chokaa ambayo yamepondwa, hivi kwamba miti mitakatifu[n] na vinara vya uvumba havitasimama.[o] **10** Kwa maana jiji lenye ngome litakuwa peke yake, uwanja wa malisho utaachwa peke yake na kuachwa kama nyika.[p] Ndama atalisha hapo, naye atalala hapo; naye kwa kweli atakula matawi yake.[q] **11** Vitawi vyake vitakapokuwa vimekauka, wanawake wanaoingia watavivunja, na kuviwasha.[a] Kwa maana wao ni kundi la watu lisilo na hamu ya uelewaji.[b] Ndiyo sababu Mtengenezaji wake hatalionyesha rehema, na Mfanyizaji wake hatalionyesha kibali.[c]

12 Na itatukia katika siku ile kwamba Yehova atayapiga matunda,[d] kuanzia kijito kinachotiririka cha ule Mto[e] mpaka kwenye bonde la mto la Misri,[f] na basi ninyi mtaokotwa mmoja baada ya mwingine,[g] enyi wana wa Israeli. **13** Na itatukia katika siku ile kwamba baragumu kubwa itapigwa,[h] na wale wanaoangamia katika nchi ya Ashuru[i] na wale waliotawanyika katika nchi ya Misri[j] hakika watakuja na kumwinamia[k] Yehova kwenye mlima mtakatifu katika Yerusalemu.[l]

28 Ole wake taji lenye utukufu la walevi wa Efraimu,[m] na ua linalonyauka la pambo lake la uzuri lililo juu ya kichwa cha bonde lenye rutuba la wale ambao divai imewashinda nguvu! **2** Tazama! Yehova ana mtu mwenye nguvu na aliye hodari.[n] Hakika atatupa chini kwa nguvu kama dhoruba ya mawe yenye mngurumo,[o] dhoruba yenye kuangamiza, kama dhoruba yenye mngurumo ya maji yenye nguvu, yanayofurika.[p] **3** Mataji yenye utukufu ya walevi wa Efraimu yatakanyagiwa[q] chini kwa miguu. **4** Na ua linalonyauka[r] la pambo lake la uzuri lililo juu ya kichwa cha bonde lenye rutuba litakuwa kama

SURA 27
a Kum 33:29; 1Sa 2:9
b Isa 35:6; Isa 41:18; Isa 58:11
c Zb 121:4; Isa 46:4
d Zb 85:3; Zb 103:9; Isa 12:1
e Lu 6:44
f 2Sa 23:6; Isa 10:17; Ebr 6:8
g Isa 57:19; Eze 34:25; Ho 2:18; Ro 5:1; 2Ko 5:19
h Eze 39:25
i Zb 92:13; Isa 37:31; Isa 60:22; Yer 30:19; Ho 14:5
j Isa 10:20; Yer 50:33
k Yer 4:11; Eze 13:13
l Isa 4:4; Isa 48:10; Eze 24:13
m Ro 11:26
n Isa 17:8; Mik 5:13
o 2Nya 34:4
p Isa 6:11; Isa 17:9; Yer 26:18; Omb 2:5; Eze 36:4
q Isa 7:25; Isa 17:2; Isa 32:14

Safu ya 2
a Zb 80:16; Isa 6:13; Eze 15:6; Mt 3:10; Yoh 15:6
b Kum 32:28; Isa 1:3; Yer 4:22; Ho 4:6
c 2Nya 36:16; Eze 9:10; 2Th 1:8
d Isa 11:11; Isa 24:13
e Yos 24:2
f Hes 34:5; 1Fa 8:65
g Kum 30:3; Ne 1:9; Yer 3:14; Amo 9:14; Lu 15:4
h Isa 11:12; Isa 49:22; Isa 62:10
i 2Fa 17:6; Isa 11:16; Ho 9:3
j Yer 43:7; Ho 8:13; Zek 10:10
k Zb 95:6; Zek 14:16
l Zb 122:4; Isa 2:3; Isa 25:6; Isa 52:1; Yer 3:17

SURA 28 **m** Isa 7:2; Ho 7:11; **n** Isa 7:17; Isa 7:20; **o** Ayu 38:22; Isa 28:17; Eze 13:11; **p** Isa 29:6; Nah 1:8; **q** Isa 25:10; Omb 1:15; **r** Yak 1:10.

tini ya mapema[a] kabla ya wakati wa kiangazi, ambayo, wakati mwonaji anapoiona, ikiwa bado mkononi mwake, yeye huimeza.

5 Katika siku hiyo Yehova wa majeshi atakuwa kama taji la pambo[b] na kama shada la urembo[c] kwa wale wanaobaki[d] kati ya watu wake, **6** na kama roho ya haki kwa yule anayeketi katika hukumu,[e] na kama nguvu kwa wale wanaogeuzia mbali pigano kutoka katika lango.[f]

7 Na hawa pia—kwa sababu ya divai wamepotea na kwa sababu ya kileo wametangatanga. Kuhani na nabii[g]—wamepotea kwa sababu ya kileo, wamevurugika kutokana na divai, wametanga-tanga[h] kutokana na kileo; wamepotea katika kuona kwao, wameyumba-yumba kuhusu uamuzi. **8** Kwa maana meza zote zimejaa matapiko machafu[i]—hakuna mahali ambapo hayapo.

9 Mtu atamfundisha nani ujuzi,[j] na mtu atamfanya nani aelewe yale ambayo yamesikiwa?[k] Je, ni wale ambao wameachishwa kunyonya, wale walioondolewa kwenye maziwa?[l] **10** Kwa maana ni "amri juu ya amri, amri juu ya amri, kamba ya kupimia juu ya kamba ya kupimia, kamba ya kupimia juu ya kamba ya kupimia, hapa kidogo, pale kidogo."[m] **11** Kwa maana kwa njia ya wale wanaogugumiza kwa midomo yao[n] na kwa lugha tofauti[o] yeye atasema na watu hawa,[p] **12** wale ambao amewaambia: "Hapa ndipo mahali pa kupumzika. Mpeni pumziko yeye aliyechoka. Na hapa ndipo mahali pa starehe," lakini ambao hawakuwa tayari kusikia.[a] **13** Na neno la Yehova hakika litakuwa kwao "amri juu ya amri, amri juu ya amri, kamba ya kupimia juu ya kamba ya kupimia, kamba ya kupimia juu ya kamba ya kupimia,[b] hapa kidogo, pale kidogo," ili waende na hakika wajikwae kuelekea nyuma na kwa kweli wavunjwe na kunaswa na kukamatwa.[c]

14 Kwa hiyo sikieni neno la Yehova, ninyi wenye kujigamba, ninyi watawala[d] wa watu hawa walio katika Yerusalemu: **15** Kwa sababu mmesema: "Tumefanya agano pamoja na Kifo;[e] nasi tumetekeleza maono pamoja na Kaburi;*[f] lile furiko la ghafula linalofurika, ikiwa litapita katikati, halitatufikia, kwa maana tumefanya uwongo kuwa kimbilio[g] letu nasi tumejificha katika jambo lisilo la kweli";[h] **16** kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Tazama, ninaweka katika Sayuni[i] jiwe[j] kuwa msingi, jiwe lililojaribiwa,[k] jiwe la pembeni[l] lenye thamani la msingi imara.[m] Yeyote anayeonyesha imani hataingiwa na wasiwasi.[n] **17** Nami nitaifanya haki kuwa kamba ya kupimia[o] na uadilifu[p] kuwa timazi; na mvua ya mawe[q] itafagilia mbali lile kimbilio la uwongo,[r] na maji yatafurika mahali pa maficho.[s] **18** Na lile agano lenu pamoja na Kifo hakika litavunjwa,[t] na yale maono yenu pamoja na Kaburi* hayatasimama.[u] Lile furiko la ghafula linalofurika, wa-

SURA 28

a Yer 24:2
Nah 3:12
jia,[j] na kusema: **2** “Ne-
nda, ukaite masikioni mwa Ye-
rusalemu, ukisema, ‘Yehova
amesema hivi:[k] “Ninakumbu-
ka vema fadhili zako zenye
upendo wakati wa ujana wako,[l]
upendo wako wakati ulipochu-
mbiwa ili kuolewa,[m] ulivyo-
tembea kunifuata nyikani, ka-
tika nchi ambayo haipandwi
mbegu.[n] **3** Israeli alikuwa
kitu kitakatifu kwa Yehova,[o]
zao la kwanza kwake Yeye.”’[p]
‘Watu wowote waliomrarua
walikuwa wakijiingiza katika
hatia.[q] Msiba ulikuwa ukija juu
yao,’ alisema Yehova.”[r]
4 Lisikie neno la Yehova, Ee
nyumba ya Yakobo,[s] nanyi nyo-
te familia za nyumba ya Isra-
eli.[t] **5** Yehova amesema hivi:
“Baba zenu walipata jambo
gani ndani yangu ambalo ha-
likuwa la haki,[u] hivi kwamba

SURA 1

a Isa 2:8
Mdo 7:41
b 1Fa 18:46
2Fa 4:29
2Fa 9:1
Ayu 38:3
Lu 12:37
1Pe 1:13
c Yos 1:9
Eze 2:6
d Yer 15:20
e Yer 20:11
Eze 3:8
Mik 3:8
f Yer 26:12
Da 9:6
g Zb 129:2
h Mwa 28:15
Kut 3:12
Yos 1:5
i Yer 15:20
Ro 8:31

SURA 2

j Ebr 1:1
k Isa 37:33
l Eze 16:8
Ho 2:15
m Kut 24:3
n Kum 2:7
Ne 9:12
o Kut 19:6
Kum 7:6
p Yak 1:18
Ufu 14:4
q Isa 41:11
Zek 1:15
r Kut 17:13
s Yer 5:20
t Ho 4:1
u Isa 5:4
Mik 6:3

Safu ya 2

a Yer 12:2
b Kum 32:21
1Fa 16:26
2Fa 17:15
Mdo 14:15
c Zb 115:8
d Kut 14:30
Amu 6:13
Isa 63:11
Ho 13:4
e Kum 1:1
Kum 32:10
f Kum 8:15
Ne 9:20
g Zb 23:4
h Hes 13:27
Kum 6:11
Kum 8:7
Ne 9:25
i Law 18:24
Hes 35:33
Kum 21:23
Zb 78:58
Zb 106:38
Yer 16:18
Eze 36:17
j 1Sa 2:12
Omb 4:13
k Lu 11:52
Yoh 8:55
l Eze 34:8
m 1Fa 18:19
Yer 23:13
n 1Sa 12:21
Hab 2:18
o Eze 20:35
Mik 6:2
p Kut 20:5
q Mwa 10:4
Hes 24:24

wakasimama mbali sana nami,[a]
nao wakaendelea kufuata sa-
namu ya ubatili[b] na wao wenye-
we wakawa ubatili?[c] **6** Nao
hawakusema, ‘Yehova yuko
wapi, Yeye aliyetupandisha ku-
toka katika nchi ya Misri,[d]
Yeye aliyetutembeza kupitia
nyikani, kupitia nchi tambara-
re ya jangwani[e] na shimo, ku-
pitia nchi isiyo na maji[f] na ye-
nye kivuli kizito,[g] kupitia nchi
ambayo mwanadamu yeyote
hakupita ndani yake na amba-
yo hakuna mtu wa udongo ali-
yekaa ndani yake?’
7 “Nami mwishowe nikawa-
leta ninyi katika nchi yenye
mashamba ya matunda, ili mle
matunda yake na vitu vyake
vyema.[h] Lakini mkaingia na
kuitia unajisi nchi yangu; na-
nyi mkaufanya urithi wangu
kuwa chukizo.[i] **8** Makuhani
wenyewe hawakusema, ‘Yeho-
va yuko wapi?’[j] Na wale wa-
naoshughulika na sheria ha-
wakunijua;[k] na wachungaji we-
nyewe walinikosea,[l] na hata
manabii walitoa unabii kupitia
Baali,[m] nao wakawafuata wale
ambao hawangeweza kuleta
faida yoyote.[n]
9 “‘Kwa hiyo nitapambana
zaidi nanyi,’[o] asema Yehova,
‘nami nitapambana na wana
wa wana wenu.’[p]
10 “‘Lakini vukeni mpaka
nchi za pwani za Kitimu,[q] mka-
one. Ndiyo, tumeni watu Ke-
dari[r] nanyi mfikirie kwa njia
ya pekee, mkaone ikiwa jambo
lolote kama hili limetendeka.[s]
11 Je, taifa limebadili miu-
ngu,[t] kwa ajili ya ile ambayo si
miungu?[u] Lakini watu wangu

r Mwa 25:13; Zb 120:5; Yer 49:28; s Yer 18:13; t Mik 4:5; u Zb 115:4; Isa 37:19; Yer 16:20; 1Ko 8:4.

mwenyewe wameubadili utu-
kufu wangu kwa ajili ya kitu
ambacho hakiwezi kuleta faida yoyote.[a] **12** Tazameni kwa
mshangao, enyi mbingu, jambo
hili; na nywele zisimame kwa
woga mkubwa sana,' asema Yehova,[b] **13** 'kwa sababu kuna
mambo mawili mabaya ambayo
watu wangu wamefanya: Wameniacha mimi,[c] niliye che-
mchemi ya maji yaliyo hai,[d] ili
wajichimbie matangi ya maji,
matangi yaliyovunjika, amba-
yo hayawezi kutunza maji.'

14 "'Je, Israeli ni mtumi-
shi,[e] au ni mtumwa aliyezaliwa
nyumbani? Kwa nini amekuwa
kitu cha kuporwa? **15** Wana-
simba wenye manyoya shingo-
ni wananguruma[f] juu yake; wa-
metoa sauti zao.[g] Nao wakaifa-
nya nchi yake kuwa kitu cha
kushangaza. Majiji yake yame-
washwa moto, hivi kwamba ha-
kuna mkaaji.[h] **16** Hata wana
wa Nofu[i] na Tahpanesi[j] walien-
delea kujilisha juu yako kwe-
nye utosi wa kichwa.[k] **17** Je,
hilo silo jambo ulilojifanyia
mwenyewe kwa kumwacha Ye-
hova Mungu[l] wako wakati ali-
pokuwa akikutembeza njia-
ni?[m] **18** Na sasa kwa nini uji-
shughulishe na njia ya Misri[n]
ili kunywa maji ya Shihori?[o]
Na kwa nini ujishughulishe
na njia ya Ashuru[p] ili kunywa
maji ya ule Mto? **19** Ubaya
wako unapaswa kukurekebi-
sha,[q] na matendo yako mwe-
nyewe ya kukosa uaminifu ya-
napaswa kukukaripia.[r] Jua,
basi, na kuona kwamba ku-
mwacha Yehova Mungu wako
ni jambo baya na lenye uchu-
ngu,[s] nawe hujaingiwa na hofu
yangu,'[t] asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu,[a] Yehova wa majeshi.

20 "'Kwa maana zamani ni-
livunja nira yako vipande-vi-
pande;[b] nilizikata pingu zako.
Lakini ulisema: "Mimi sita-
tumikia," kwa maana uliku-
wa umelala huku umejinyoo-
sha[c] juu ya kila kilima kirefu
na chini ya kila mti wenye ma-
jani mengi,[d] ukifanya ukaha-
ba.[e] **21** Lakini mimi nilikuwa
nimekupanda kama mzabi-
bu bora mwekundu,[f] wote uki-
wa mbegu ya kweli. Basi ni
jinsi gani umebadilika kuniele-
kea ukawa machipukizi yaliyo-
haribika ya mzabibu wa kige-
ni?'[g]

22 "'Lakini hata ukijiosha
kwa magadi na kujichuku-
lia kiasi kikubwa cha sabu-
ni,[h] kosa lako hakika lingeku-
wa doa mbele zangu,'[i] asema
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova. **23** Jinsi gani unaweza
kusema, 'Mimi sikujitia unaji-
si.[j] Sikufuata Mabaali'?[k] Ona
njia yako katika bonde.[l] Anga-
lia lile ambalo umefanya. Nga-
mia-jike mchanga aliye mwe-
pesi ambaye anakimbia huku
na huku bila mwelekeo kati-
ka njia zake; **24** punda-mi-
lia[m] aliyezoea nyika, wakati
wa tamaa ya nafsi yake, akiu-
pumua upepo;[n] wakati wake
wa kupandwa, ni nani anaye-
weza kumgeuza? Wale wote
wanaomtafuta hawatajicho-
sha. Watampata katika mwe-
zi wake. **25** Zuia mguu wako
usiwe mguu wazi, na koo yako
isiwe na kiu.[o] Lakini ulisema,
'Hakuna matumaini![p] Hapana,
lakini mimi nimewapenda wa-
geni,[q] nami nitawafuata.'[r]

SURA 2

a Zb 106:20
Ho 4:7
Ro 1:23
b Isa 1:2
Yer 6:19
c Amu 10:13
1Sa 12:10
d Zb 36:9
Yer 17:13
Yoh 17:3
Ufu 22:1
e Kut 4:22
Isa 41:8
f Isa 5:29
g Eze 5:14
h Yer 4:7
Yer 9:11
Sef 3:6
i Isa 19:13
Yer 44:1
Yer 46:19
Eze 30:13
j Yer 43:7
Yer 46:14
Eze 30:18
k Isa 1:7
l 1Nya 28:9
2Nya 7:19
m Kum 32:10
Zb 77:20
Zb 78:54
Zb 136:16
Isa 63:13
n Isa 30:2
Isa 31:1
Omb 5:6
Eze 16:26
Eze 17:15
Eze 23:3
2Ko 6:14
o Yos 13:3
Isa 23:3
p 2Fa 16:7
Ho 5:13
q Isa 3:9
Ho 5:5
r Ho 11:7
s Yer 4:18
Amo 8:10
t Yer 5:22

Safu ya 2

a Mdo 4:24
b Law 26:13
Kum 4:20
Isa 9:4
Nah 1:13
c Isa 57:5
Yer 3:6
Yer 17:2
d 1Fa 14:23
Eze 6:13
Ho 4:13
e Kut 34:15
Eze 16:15
Ho 6:10
f Kut 15:17
Zb 44:2
Zb 80:8
Isa 5:1
g Isa 1:21
Isa 5:4
h Ayu 9:30
i Kum 32:34
Ayu 14:17
Zb 90:8
Yer 16:17
Ho 13:12
Amo 8:7
j Met 28:13
Met 30:12
k Met 30:20
l Yer 7:31
m Ho 8:9
n Yer 14:6
o Ho 2:3

p Yer 18:12; q Isa 2:6; Yer 3:13; r Yer 44:17.

26 "Watu wa nyumba ya Israeli wameona aibu kama ile ya mwizi ambaye amekamatwa,[a] wao, wafalme wao, wakuu wao na makuhani wao na manabii wao.[b] **27** Wanauambia mti, 'Wewe ni baba yangu,'[c] na jiwe, 'Wewe ulinizaa.' Lakini mimi wamenigeuzia sehemu ya nyuma ya shingo badala ya uso.[d] Na wakati wa msiba wao watasema, 'Simama utuokoe!'[e]

28 "Lakini iko wapi miungu yako ambayo umejifanyia?[f] Na isimame ikiwa inaweza kukuokoa wakati wa msiba wako.[g] Kwa maana miungu yako imekuwa kama hesabu ya majiji yako, Ee Yuda.[h]

29 "'Kwa nini mnaendelea kushindana nami?'[i] Kwa nini nyote mmenikosea?'[j] asema Yehova. **30** Nimewapiga wana wenu bila matokeo.[k] Hawakushika nidhamu yoyote.[l] Upanga wenu umewala manabii wenu, kama simba anayeangamiza.[m] **31** Enyi kizazi, oneni wenyewe neno la Yehova.[n]

"Je, nimekuwa nyika tupu kwa Israeli[o] au nchi yenye giza zito? Kwa nini hawa, watu wangu, wamesema, 'Tumeenda huku na huku. Hatutakuja kwako tena'?[p] **32** Je, bikira anaweza kuyasahau mapambo yake, na bibi-arusi mavazi yake ya kifuani? Lakini watu wangu mwenyewe—wamenisahau mimi kwa muda wa siku zisizo na hesabu.[q]

33 "Kwa nini wewe, Ee mwanamke, unaboresha njia yako ili kutafuta upendo? Kwa hiyo pia umefundisha njia zako mambo mabaya.[r] **34** Pia, alama za damu za nafsi[s] za maskini wasio na hatia[t] zimepatikana katika pindo za nguo zako. Sikuzipata katika tendo la kuvunja na kuingia, lakini ziko juu ya hizo zote.[a]

35 "Lakini unasema, 'Nimebaki bila hatia. Hakika hasira yake imeondoka juu yangu.'[b]

"Tazama, ninaingia katika ugomvi pamoja nawe kwa sababu unasema, 'Sikutenda dhambi.'[c] **36** Kwa nini unaona kubadili njia yako kuwa jambo dogo sana?[d] Utaona aibu kwa ajili ya Misri,[e] kama vile ulivyoona aibu kwa ajili ya Ashuru.[f] **37** Kwa sababu hiyo pia utaenda mikono yako ikiwa juu ya kichwa chako,[g] kwa sababu Yehova amevikataa vitu vyako ambavyo una uhakika ndani yake, nawe hutapata mafanikio katika hivyo."

3 Kuna msemo: "Mwanamume akimwacha mke wake na mke huyo aondoke kwake na kuwa wa mwanamume mwingine, je, mwanamume huyo anapaswa kurudi kwake tena?"[h]

Je, nchi hiyo haikutiwa unajisi hakika?[i]

"Nawe mwenyewe umefanya ukahaba pamoja na rafiki wengi;[j] na je, unapaswa kurudi kwangu mimi?"[k] asema Yehova. **2** "Inua macho yako kuelekea mapito yaliyokanyagwa, ukaone.[l] Ni wapi ambapo hawakukulala kinguvu?[m] Umekaa kando ya njia kwa ajili yao, kama Mwarabu nyikani;[n] nawe unaendelea kuitia nchi unajisi kwa matendo yako ya ukahaba na kwa ubaya wako.[o] **3** Kwa hiyo manyunyu mengi yamezuiwa,[p] na hata mvua ya ma-

SURA 2

a Kut 22:7
b Ezr 9:7
Da 9:6
c Isa 44:13
Hab 2:18
d 2Nya 29:6
Yer 32:33
e Amu 10:15
2Nya 20:9
Zb 78:34
Zb 106:47
Isa 26:16
Ho 5:15
f Kum 32:37
Amu 10:13
Isa 45:20
g Amu 10:14
Isa 46:7
h Yer 11:13
i 1Sa 2:10
j Yer 5:1
Yer 9:2
Da 9:11
Ho 7:13
k 2Nya 28:22
Isa 9:13
l Isa 1:5
Yer 5:3
Sef 3:2
m 2Nya 36:16
Ne 9:26
Mt 21:35
Mt 23:34
Mdo 7:52
1Th 2:15
n Mik 6:9
o 2Nya 31:10
Ne 9:25
p Kum 32:15
q Zb 106:21
Isa 17:10
Yer 13:25
Yer 18:15
Ho 8:14
r 2Nya 33:9
s Mwa 9:5
t 2Fa 21:16
2Fa 24:4
Zb 106:38
Isa 10:2
Isa 59:7
Yer 19:4
Mt 23:35

Safu ya 2

a Kut 22:2
b Met 28:13
c 1Yo 1:8
d Ho 12:2
e Isa 30:3
Yer 37:7
f 2Nya 28:20
g 2Sa 13:19

SURA 3

h Kum 24:4
i Isa 24:5
Yer 2:7
j Yer 2:20
Eze 16:28
k Yer 4:1
Zek 1:3
l Yer 2:23
m Eze 16:16
Eze 20:28
n Mwa 38:16
Met 23:28
o Yer 2:7

p Law 26:19; Kum 28:23; Isa 5:6; Yer 9:12; Yer 14:4; Amo 4:7; Hag 1:11.

sika haikunyesha.[a] Nawe umekuwa na paji la uso la mke anayefanya ukahaba. Umekataa kufedheheka.[b] **4** Je, umeniita kutoka sasa na kuendelea
‘Baba yangu,[c] wewe ni rafiki
wa karibu wa ujana wangu![d]
5 Je, mtu anapaswa kufungia
kinyongo mpaka wakati usio na kipimo, au kuendelea kuangalia jambo milele?’[e] Tazama! Umesema, nawe ukaendelea kufanya mambo mabaya na kupata ushindi.”[f]

6 Na Yehova akaniambia katika siku za mfalme Yosia:[g] “‘Je, umeona lile ambalo Israeli asiye mwaminifu amefanya?[h] Anaenda juu ya kila mlima mrefu[i] na chini ya kila mti wenye majani mengi,[j] ili afanye ukahaba huko.[k] **7** Na baada ya yeye kufanya mambo hayo yote niliendelea kusema kwamba arudi kwangu, lakini hakurudi;[l] na Yuda akaendelea kumtazama dada yake mwenye hila.[m] **8** Nilipoona jambo hilo, kwa sababu Israeli asiye mwaminifu alikuwa amefanya uzinzi, nilimfukuza[n] nami nikampa cheti chake cha talaka kamili,[o] ingawa hivyo Yuda, dada yake anayetenda kwa hila, hakuogopa, bali yeye mwenyewe pia akaanza kwenda na kufanya ukahaba.[p] **9** Na ukahaba wake ulifanyika kwa sababu ya maoni yake ya kipuuzi, naye aliendelea kuitia nchi unajisi[q] na kufanya uzinzi pamoja na mawe na pamoja na miti;[r] **10** na hata ijapokuwa hayo yote Yuda dada yake mwenye hila hakurudi kwangu kwa moyo[s] wake wote, ila kwa uwongo,’[t] asema Yehova.”

SURA 3

a Yer 5:24
b Yer 6:15
Sef 3:5
c Yer 3:19
Yer 31:9
d Zb 71:5
Met 2:17
Yer 2:2
Ho 2:15
e Zb 77:7
Zb 103:9
Isa 57:16
Isa 64:9
f Mik 2:1
Mik 7:3
Sef 3:3
g 2Fa 22:1
h Yer 7:24
i Isa 57:7
Yer 2:20
Eze 6:3
j 1Fa 14:23
Yer 17:2
k Eze 20:28
Ho 4:13
l 2Fa 17:13
2Nya 30:6
Ho 14:1
m Eze 16:46
Eze 23:2
n Isa 1:21
Eze 23:9
Ho 2:2
Ho 9:15
o Kum 24:1
Isa 50:1
p 2Fa 17:19
Eze 23:11
q Yer 2:7
r Isa 57:6
Yer 2:27
s Zb 78:37
Ho 7:14
t Met 11:20

Safu ya 2

a Eze 16:51
Eze 23:11
b 2Fa 17:6
Yer 23:8
Yer 31:8
c Yer 4:1
Eze 33:11
Ho 6:1
Ho 14:1
d Ho 11:8
e 2Sa 22:26
Zb 18:25
Zb 86:5
Ufu 15:4
f Zb 79:5
g Law 26:40
Met 28:13
Ho 7:13
h Yer 2:25
Eze 16:15
i Kum 12:2
j Isa 57:17
Yer 4:22
k Isa 54:5
Yer 2:2
Yer 31:32
Ho 2:19
l Yer 23:3
Ro 11:5
m Yer 23:4
Eze 34:23
Efe 4:11
n Yoh 21:15
Mdo 20:28
o Isa 61:4
Ho 1:10
p 1Sa 4:5
q Isa 65:17

11 Na Yehova akaendelea kuniambia: “Israeli asiye mwaminifu ameonyesha nafsi yake kuwa yenye uadilifu kuliko Yuda anayetenda kwa hila.[a] **12** Nenda, nawe uitangazie kaskazini[b] maneno haya na kusema:

“‘“Rudi, Ee Israeli mwenye kuasi,” asema Yehova.’[c] ‘“Sitawatazama ninyi kwa hasira,[d] kwa maana mimi ni mshikamanifu,”[e] asema Yehova.’ ‘“Sitaendelea kufungia kinyongo mpaka wakati usio na kipimo.[f] **13** Ila uangalie tu kosa lako, kwa maana umemkosea Yehova Mungu wako.[g] Nawe umeendelea kutawanya njia zako kwa wageni[h] chini ya kila mti wenye majani mengi,[i] lakini ninyi hamkuisikiliza sauti yangu,” asema Yehova.’”

14 “Rudini, enyi wana waasi,’[j] asema Yehova. “Kwa maana mimi nimekuwa mume wenu;[k] nami nitawachukua, mmoja kutoka katika jiji moja na wawili kutoka katika familia moja, nami nitawaleta ninyi Sayuni.[l] **15** Nami nitawapa wachungaji wenye kupatana na moyo wangu,[m] na hakika wao watawalisha ninyi kwa ujuzi na ufahamu.[n] **16** Na itatukia kwamba mtakuwa wengi nanyi hakika mtazaa matunda katika nchi siku hizo,” asema Yehova.[o] “Hawatasema tena, ‘Sanduku la agano la Yehova!’[p] wala halitaingia moyoni, wala hawatalikumbuka[q] au kulitamani, nalo halitafanywa tena. **17** Wakati huo wataita Yerusalemu kuwa kiti cha ufalme cha Yehova;[r] na mataifa yote yataletwa

r Zb 87:3; Yer 14:21; Eze 43:7.

pamoja[a] kwake kwa jina la Yehova katika Yerusalemu,[b] nao hawataufuata tena ukaidi wa moyo wao mbaya."[c]

18 "Katika siku hizo watatembea, nyumba ya Yuda ikiwa kando ya nyumba ya Israeli,[d] nao pamoja[e] watatoka katika nchi ya kaskazini na kuingia katika nchi ambayo niliwapa mababu zenu kuwa fungu la urithi.[f] **19** Nami mwenyewe nimesema, 'Lo! jinsi nilivyokuweka kati ya wana na kukupa nchi yenye kutamanika,[g] fungu la urithi la pambo la majeshi ya mataifa!' Nami nikasema tena, Ninyi mtaniita '"Baba yangu!"[h] nanyi hamtarudi mwache kunifuata.' **20** 'Kwa kweli kama mke anavyomwacha mwenzake kwa hila,[i] ndivyo ninyi, enyi nyumba ya Israeli, mlivyonitendea kwa hila,'[j] asema Yehova."

21 Sauti imesikika katika njia zilizokanyagwa, kulia, kusihi kwa wana wa Israeli. Kwa maana wameipotosha njia yao;[k] wamemsahau Yehova Mungu wao.[l]

22 "Rudini, ninyi wana waasi.[m] Nitaiponya hali yenu ya uasi."[n]

"Sisi hapa! Tumekuja kwako, kwa maana wewe, Ee Yehova, ni Mungu wetu.[o] **23** Kwa kweli vilima na pia machafuko juu ya milima[p] ni uwongo.[q] Kwa kweli wokovu wa Israeli uko katika Yehova Mungu wetu.[r] **24** Lakini jambo la aibu[s] limekula kazi ya mababu zetu tangu ujana wetu, makundi yao na mifugo yao, wana wao na binti zao. **25** Tunalala katika aibu[t] yetu, na fedheha yetu inaendelea kutufunika;[a] kwa maana tumemtendea dhambi[b] Yehova Mungu wetu, sisi na baba zetu tangu ujana wetu na kuendelea mpaka leo hii,[c] nasi hatukuitii sauti ya Yehova Mungu wetu."[d]

4 "Kama ukitaka kurudi, Ee Israeli," asema Yehova, "unaweza kurudi kwangu mimi.[e] Nawe ukiondolea mbali machukizo yako kwa ajili yangu,[f] basi hutakwenda ukiwa kama mkimbizi. **2** Na hakika wewe ukiapa,[g] 'Kama anavyoishi Yehova katika kweli,[h] katika haki na katika uadilifu!'[i] ndipo kwa kweli mataifa yatajibariki katika yeye, nayo yatajisifu katika yeye."[j]

3 Kwa maana Yehova amesema hivi kwa watu wa Yuda na kwa Yerusalemu: "Jilimieni udongo unaofaa kwa kilimo, na msiendelee kupanda kati ya miiba.[k] **4** Tahiriweni kwa ajili ya Yehova, na kuondoa magovi ya mioyo yenu,[l] ninyi watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu; ili ghadhabu yangu isitoke kama moto, na hakika iteketeze bila yeyote wa kuizima, kwa sababu ya ubaya wa matendo yenu."[m]

5 Tangazeni jambo hilo katika Yuda, na kulihubiri hata katika Yerusalemu,[n] na mliseme, na kupiga baragumu katika nchi yote.[o] Iteni kwa sauti na kusema: "Jikusanyeni pamoja, nasi tuingie katika majiji yenye ngome.[p] **6** Inueni ishara kuelekea Sayuni. Andaeni mahali pa kukimbilia usalama. Msisimame tuli." Kwa ma-

SURA 3

a Isa 2:2; Isa 60:3; Mik 4:2; Zek 2:11; Zek 8:23; Ufu 7:9
b Isa 26:8; Isa 56:6; Zek 8:22
c Zb 78:8
d Yer 50:4; Ho 1:11
e 2Nya 36:23; Ezr 1:3; Eze 37:19
f Yer 23:8; Amo 9:15
g Zb 106:24; Eze 20:6
h Isa 63:16; Isa 64:8; Mt 6:8; 1Pe 1:17
i Ho 3:1
j Isa 48:8; Yer 5:11; Ho 5:7; Ho 6:7; Mal 2:11
k Met 10:9; Mik 3:9
l Isa 17:10; Eze 23:35; Ho 8:14; Ho 13:6
m Ho 6:1; Ho 14:1
n Yer 33:6; Ho 14:4
o Yer 31:18; Ho 3:5; Zek 13:9
p Isa 65:7
q Yer 10:14; Yon 2:8
r Zb 3:8; Zb 37:39; Isa 12:2; Yoh 4:22
s Yer 11:13; Ho 9:10
t Ezr 9:6; Yer 2:26; Da 9:7

Safu ya 2

a Eze 7:18
b Zb 51:4; Yer 2:19; Eze 36:31
c Ezr 9:7; Zb 106:7
d Amu 2:2; Isa 48:8; Yer 22:21; Da 9:10; 1Ko 10:8

SURA 4

e Kum 30:2; Isa 31:6; Yer 3:22; Ho 14:1; Yoe 2:12
f 2Nya 15:8
g Kum 10:20; Isa 65:16
h Isa 48:1
i Zb 99:4
j Isa 45:25; Yer 9:24; 1Ko 1:31
k Ho 10:12

l Kum 10:16; Kum 30:6; Yer 9:26; Mdo 7:51; Ro 2:29; Kol 2:11; **m** Law 26:28; Omb 4:11; **n** Yer 5:20; Yer 11:2; **o** Yer 6:1; Eze 33:3; Ho 8:1; Amo 3:6; **p** Yer 8:14; Yer 35:11.

ana kuna msiba ambao ninaleta kutoka kaskazini,[a] mshindo mkubwa. **7** Amepanda kama simba kutoka katika kichaka chake,[b] na yule anayeyaangamiza mataifa ameondoka;[c] ametoka mahali pake ili kuifanya nchi yako kuwa kitu cha kushangaza. Majiji yako yatabomoka hivi kwamba hakutakuwa na mkaaji.[d] **8** Kwa sababu hiyo vaeni nguo za magunia.[e] Pigeni vifua vyenu na kupiga mayowe,[f] kwa sababu hasira ya Yehova inayowaka haijaondoka juu yetu.[g]

9 "Na itakuwa katika siku hiyo," asema Yehova, "kwamba moyo wa mfalme utaangamia,[h] pia moyo wa wakuu; na hakika makuhani wataingiwa na mshangao, nao manabii watastaajabishwa."[i]

10 Nami nikasema: "Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Kwa kweli umewadanganya kabisa watu[j] hawa na Yerusalemu, kwa kusema, 'Mtakuwa na amani,'[k] na upanga umefika mpaka kwenye nafsi."

11 Na wakati huo watu hawa na Yerusalemu wataambiwa hivi: "Kuna upepo unaokausha wa mapito ya nyikani[l] kwenye njia ya kwenda kwa binti ya watu wangu;[m] si wa kupepeta, wala wa kusafisha. **12** Upepo unaovuma kwa nguvu kamili unatoka kwao kuja kwangu. Sasa mimi mwenyewe pia nitasema hukumu nao.[n] **13** Tazama! Atakuja kama mawingu ya mvua, na magari yake ni kama upepo wa dhoruba.[o] Farasi zake ni wepesi kuliko tai.[p] Ole wetu, kwa sababu tumeporwa! **14** Osha moyo wako uwe safi kutokana na ubaya mtupu, Ee Yerusalemu, ili upate kuokolewa.[a] Fikira zako zenye makosa zitakaa ndani yako mpaka wakati gani?[b] **15** Kwa maana sauti inasema kutoka Dani[c] nayo inatangaza jambo lenye kudhuru kutoka eneo lenye milima la Efraimu.[d] **16** Ndiyo, tangazeni jambo hilo, kwa mataifa. Lihubirini dhidi ya Yerusalemu."

"Walinzi wanakuja kutoka katika nchi ya mbali,[e] nao wataipaaza sauti yao juu ya majiji ya Yuda. **17** Wamekuwa kama walinzi wa shamba juu yake pande zote,[f] kwa sababu ameniasi hata mimi,"[g] asema Yehova. **18** "Njia yako na matendo yako—wewe utalipwa hayo.[h] Huu ndio msiba ulio juu yako, kwa maana ni mchungu; kwa sababu umefika mpaka moyoni mwako."

19 Ee matumbo yangu, matumbo yangu! Nina maumivu makali katika kuta za moyo wangu.[i] Moyo wangu umechafuka ndani yangu.[j] Siwezi kunyamaza kimya, kwa maana nafsi yangu imesikia sauti ya baragumu, king'ora cha vita.[k] **20** Mshindo juu ya mshindo umetangazwa, kwa maana nchi yote imeporwa.[l] Ghafula mahema yangu yameporwa,[m] na katika muda mfupi vitambaa vya mahema yangu. **21** Nitaendelea kuona ishara, kusikia sauti ya baragumu, mpaka wakati gani?[n] **22** Kwa maana watu wangu ni wapumbavu.[o] Hawanijali mimi.[p] Wao ni wana wasio na hekima; nao si wale

SURA 4

a Yer 1:14
Yer 6:1
Yer 21:7
Yer 25:9
b 2Fa 24:1
2Fa 25:1
Yer 5:6
Yer 50:17
c Eze 26:7
d Isa 1:7
Isa 5:9
Isa 6:11
Yer 2:15
Yer 9:11
e Yer 6:26
Yoe 2:12
Amo 8:10
f Eze 21:12
g Isa 9:17
Isa 10:4
h 2Fa 25:5
i Isa 29:9
Mdo 13:41
j Eze 14:9
2Th 2:11
k Yer 5:12
Yer 6:14
Yer 14:13
Yer 23:17
1Th 5:3
l Eze 17:10
Ho 13:15
m Isa 22:4
n Yer 1:16
o Isa 5:28
p Kum 28:49
Omb 4:19
Ho 8:1
Hab 1:8

Safu ya 2

a Isa 1:16
Eze 18:31
b Met 1:22
c Amu 18:29
Amu 20:1
Yer 8:16
d Yos 17:15
Yos 20:7
e Kum 28:49
Isa 39:3
f 2Fa 25:2
Isa 1:8
g Ne 9:26
Isa 1:20
Isa 30:9
Isa 63:10
Eze 2:3
Eze 20:21
h Zb 107:17
Met 1:31
Met 5:22
Isa 50:1
Yer 2:17
i Isa 15:5
Isa 21:3
j Zb 42:5
Isa 16:11
k Sef 1:16
l Zb 42:7
Zb 137:8
m Yer 6:26
Yer 10:20
n Yer 6:1
o Kum 32:6
Isa 6:9
Yer 5:21
p Ho 5:4

walio na uelewaji.[a] Wana hekima ya kutenda mabaya, lakini kwa kweli hawajui kutenda mema.[b]

23 Niliiona nchi, na, tazama! ilikuwa tupu na ukiwa;[c] na katika mbingu, na, tazama! nuru yake haikuwapo.[d] **24** Niliiona milima, na, tazama! ilikuwa ikitikisika, na vilima vyote vilitetemeshwa.[e] **25** Niliona, na, tazama! hapakuwa na mtu wa udongo yeyote, na viumbe vyote vinavyoruka vya mbinguni vilikuwa vimekimbia.[f] **26** Niliona, na, tazama! shamba la matunda lilikuwa nyika, na majiji yake yote yalikuwa yamebomolewa.[g] Ilikuwa kwa sababu ya Yehova, kwa sababu ya hasira yake inayowaka.

27 Kwa maana Yehova amesema hivi: "Nchi yote itakuwa mahame yenye ukiwa,[h] na je, mimi sitafanya maangamizi kamili?[i] **28** Kwa sababu nchi hiyo itaomboleza,[j] na mbingu juu hakika zitakuwa na giza.[k] Ni kwa sababu nimesema, nimefikiria, wala sikujuta, wala sitarudi nyuma kutoka katika jambo hilo.[l] **29** Kwa sababu ya sauti ya wapanda-farasi na wapiga-upinde jiji zima linakimbia.[m] Wameingia vichakani, nao wamepanda kuingia ndani ya miamba.[n] Kila jiji limeachwa, na hakuna mtu anayekaa ndani yake."

30 Sasa kwa kuwa umeporwa, utafanya nini, kwa sababu ulikuwa ukivaa nguo nyekundu, kwa sababu ulikuwa ukijipamba kwa mapambo ya dhahabu, kwa sababu ulikuwa ukipanua macho yako kwa kujipaka wanja?[a] Ulikuwa ukijirembesha kwa ubatili tu.[b] Wale wanaokutamani wamekukataa; wanaendelea kuitafuta nafsi yako.[c] **31** Kwa maana nimeisikia sauti kama ya mwanamke mgonjwa, taabu kama ya mwanamke anayezaa mtoto wake wa kwanza,[d] sauti ya binti Sayuni ambaye anaendelea kuvuta pumzi kwa nguvu. Anaendelea kuinyoosha mikono yake:[e] "Ole wangu, sasa, kwa maana nafsi yangu imechoka kwa sababu ya wauaji!"[f]

5 Nendeni huku na huku katika barabara za Yerusalemu na mwone, sasa, na mjue, nanyi mjitafutie katika viwanja vyake vya watu wote ikiwa mnaweza kumpata mwanadamu,[g] ikiwa kuna yeyote anayetenda haki,[h] yeyote anayetafuta uaminifu,[i] nami nitamsamehe. **2** Hata wakisema: "Kama anavyoishi Yehova!" watakuwa wanaapa kwa uwongo mtupu.[j]

3 Ee Yehova, je, macho yako hayaangalii uaminifu?[k] Umewapiga,[l] lakini hawakuwa wagonjwa.[m] Uliwaangamiza.[n] Walikataa kukubali nidhamu.[o] Walizifanya nyuso zao kuwa ngumu kuliko mwamba.[p] Walikataa kurudi.[q] **4** Hata kama mimi mwenyewe nikisema: "Hakika wao ni wa tabaka ya chini. Walitenda kwa upumbavu, kwa maana wameipuuza njia ya Yehova, hukumu ya Mungu wao.[r] **5** Nitashika njia kwenda kwa wakuu na kusema nao;[s] kwa maana wao lazima waliiangalia njia ya Yehova, hukumu ya Mungu wao.[t] Haki-

SURA 4

a Ho 4:14
b Mik 2:1
c Isa 24:19; Yer 9:10
d Isa 5:30; Isa 13:10; Eze 32:8; Yoe 2:31; Mt 24:29
e Isa 5:25; Eze 38:20; Nah 1:5; Hab 3:6
f Yer 9:10; Ho 4:3; Sef 1:3
g Kum 29:23
h 2Nya 36:21; Isa 6:11; Yer 12:11; Eze 33:28
i Law 26:32; Yer 10:22; Yer 12:11; Eze 11:13
j Isa 24:4; Ho 4:3; Yoe 1:10
k Isa 5:30; Isa 50:3; Yoe 2:2; Yoe 2:30
l Hes 23:19; 2Fa 23:26; Isa 43:13; Isa 46:10; Eze 24:14
m 2Fa 25:4
n Isa 2:19; Ufu 6:15

Safu ya 2

a 2Fa 9:30; Eze 23:40; Ufu 17:4
b Eze 23:26
c Yer 22:20; Omb 1:2; Ufu 17:16
d Yer 6:24; 1Th 5:3
e Isa 1:15; Omb 1:17
f Yer 45:3; Eze 23:47

SURA 5

g Eze 22:30
h Mwa 18:32; Zb 12:1; Zb 14:3; Eze 22:29; Amo 5:7; Mik 7:2
i Isa 59:4
j Isa 48:1; Yer 7:9
k 2Nya 16:9; Zb 101:6
l 2Nya 28:22
m Isa 1:5; Isa 9:13; Yer 2:30
n Kum 28:21
o Zb 50:17; Isa 1:5; Isa 42:25; Yer 7:28; Sef 3:2
p Met 21:29; Zek 7:11
q Eze 3:7
r Isa 27:11; Yer 7:8; Ho 4:6

s Mal 2:7; t Mik 3:1.

ka wao wote pamoja lazima waliivunja nira; lazima wawe walizikata pingu."[a]

6 Ndiyo sababu simba kutoka msituni amewashambulia, mbwa-mwitu wa nchi tambarare za jangwani anaendelea kuwapora,[b] chui anakaa macho kwenye majiji yao.[c] Kila mtu anayetoka humo anararuliwa vipande-vipande. Kwa maana makosa yao yamekuwa mengi; matendo yao ya kukosa uaminifu yamekuwa mengi sana.[d]

7 Nawezaje kukusamehe kwa ajili ya jambo hili? Wana wako wameniacha, nao wanaendelea kuapa[e] kwa kitu ambacho si Mungu.[f] Nami niliendelea kuwashibisha,[g] lakini wakaendelea kufanya uzinzi,[h] nao wanaenda katika nyumba ya mwanamke kahaba wakiwa makundi-makundi. **8** Wamekuwa farasi walioshikwa na nyege, wenye mapumbu yenye nguvu. Kila mmoja wao analia kwa ajili ya mke wa mwenzake.[i]

9 "Je, nisitoze hesabu kwa sababu ya mambo haya?" asema Yehova.[j] "Au, je, nafsi yangu isijilipizie kisasi juu ya taifa ambalo liko hivyo?"[k]

10 "Njooni juu ya mistari yake ya mizabibu na kuharibu,[l] lakini msiangamize kabisa.[m] Chukueni machipukizi yake yenye kutoa majani mengi, kwa maana hayo si ya Yehova.[n] **11** Kwa maana nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda hakika zimenitendea kwa hila," asema Yehova.[o] **12** "Wamemkana Yehova, nao wanaendelea kusema, 'Yeye hayuko.[p] Na hakuna msiba utakaokuja juu yetu, nasi hatutaona upanga wala njaa.'[a] **13** Nao manabii wanakuwa upepo, na lile neno halimo ndani yao.[b] Hivyo ndivyo watakavyotendewa."

14 Kwa hiyo Yehova, Mungu wa majeshi, amesema hivi: "Kwa sababu ninyi mnasema jambo hilo, tazama, nayafanya maneno yangu kinywani mwenu kuwa moto,[c] na watu hawa watakuwa kuni, nao hakika utawateketeza."[d]

15 "Tazama, ninaleta juu yenu taifa kutoka mbali,[e] enyi nyumba ya Israeli," asema Yehova. "Ni taifa linalodumu. Ni taifa la zamani za kale,[f] taifa ambalo lugha yake hamwijui, nanyi hamwezi kusikia na kuelewa yale wanayosema. **16** Podo lao ni kama kaburi lililo wazi; wote ni wanaume wenye nguvu.[g] **17** Hakika wao pia watakula mavuno yako na mkate wako.[h] Watu hao watakula wana wako na binti zako. Watakula makundi yako na mifugo yako. Watakula mzabibu wako na mtini wako.[i] Watavunja-vunja kwa upanga majiji yako yenye ngome unayoyategemea."

18 "Na hata katika siku hizo," asema Yehova, "Sitawaangamiza ninyi.[j] **19** Na itakuwa kwamba mtasema, 'Kwa sababu gani Yehova Mungu wetu ametutendea mambo haya yote?'[k] Nawe utawaambia, 'Kama mlivyoniacha mimi, kwenda kumtumikia mungu wa kigeni katika nchi yenu, ndivyo mtakavyowatumikia wageni katika nchi ambayo si yenu.'"[l]

20 Tangazeni jambo hili katika nyumba ya Yakobo, na

SURA 5

a Zb 2:3
b Zb 104:20
Sef 3:3
c Ho 13:7
d Ezr 9:6
Isa 59:12
Eze 23:19
e Yos 23:7
Yer 12:16
Amo 8:14
Sef 1:5
f Kum 32:21
Yer 2:11
1Ko 8:4
Ga 4:8
g Eze 16:49
Ho 13:6
h Eze 22:11
i Yer 13:27
j Yer 9:9
k Law 26:25
Yer 44:22
Nah 1:2
l 2Nya 36:17
Yer 39:8
m Law 26:44
Yer 46:28
Amo 9:8
n Zb 78:61
o Isa 48:8
Yer 3:20
Ho 5:7
Ho 6:7
p 2Nya 36:16
Isa 28:15

Safu ya 2

a Zb 10:6
Yer 4:10
Yer 23:17
b Isa 41:29
Ho 9:7
c Yer 1:9
d Yer 23:29
Ho 6:5
Ufu 11:5
e Kum 28:49
Yer 1:15
Yer 4:16
Yer 25:9
Eze 7:24
f Hab 1:6
g Kum 28:50
h Law 26:16
Kum 28:51
i Yer 8:13
j Yer 4:27
k Kum 29:25
1Fa 9:9
Yer 2:35
Yer 13:22
Yer 16:10
l Kum 4:27
Kum 28:48
2Nya 7:22

kulitangaza katika Yuda, mkisema: **21** "Sikieni jambo hili, sasa, enyi watu wasio na hekima ambao hawana moyo wa ufahamu:[a] Wana macho, lakini hawawezi kuona;[b] wana masikio, lakini hawawezi kusikia.[c] **22** 'Je, hata hamniogopi mimi,'[d] asema Yehova, 'au, je, hata hamna maumivu makali kwa sababu yangu,[e] ambaye nimeweka mchanga kuwa mpaka wa bahari, sharti linalodumu mpaka wakati usio na kipimo kwamba haiwezi kuvuka? Ingawa mawimbi yake husukasuka, bado hayawezi kushinda; na ingawa huchafuka, bado hayawezi kuuvuka.[f] **23** Lakini hawa watu wamekuwa na moyo mgumu na wenye kuasi; wamegeuka kando nao wanaendelea kutembea katika mwendo wao.[g] **24** Lakini hawakusema moyoni mwao: "Sasa, na tumwogope Yehova Mungu wetu,[h] Yeye anayenyesha mvua kubwa na mvua ya vuli na mvua ya masika katika majira yake,[i] Yeye anayetulindia majuma yaliyoamriwa ya mavuno."[j] **25** Makosa yenu wenyewe yameyafukuzia mbali mambo hayo, na dhambi zenu wenyewe zimewazuilia ninyi mema.[k]

26 "'Kwa maana watu waovu wamepatikana kati ya watu wangu.[l] Wanaendelea kukaza macho, kama wakati wawindaji wa ndege wanapochutama.[m] Wameweka mtego wenye kuharibu. Wao wanawanasa watu. **27** Kama tundu lilivyojaa viumbe vinavyoruka, ndivyo nyumba zao zilivyojaa udanganyifu.[n] Ndiyo sababu wamekuwa wakuu nao wanapata utajiri.[a] **28** Wamenenepa;[b] wameng'aa. Pia wamejaa kabisa mambo mabaya. Hawakutetea kesi yoyote,[c] hata kesi ya mvulana asiye na baba,[d] ili wapate mafanikio;[e] nao hawakuifuatilia hukumu ya maskini.'"

29 "Je, nisitoze hesabu kwa sababu ya mambo hayo," asema Yehova, "au, je, nafsi yangu isijilipizie kisasi juu ya taifa ambalo liko hivyo?[f] **30** Hali yenye kushangaza, ndiyo, jambo lenye kuchukiza sana, limetokezwa katika nchi:[g] **31** Manabii wenyewe kwa kweli wanatoa unabii kwa uwongo;[h] nao makuhani wanakandamiza kulinganana na nguvu zao.[i] Na watu wangu wamependa mambo yawe hivyo;[j] nanyi mtafanya nini mwisho wake?"[k]

6 Kimbilieni usalama, enyi wana wa Benyamini, kutoka katikati ya Yerusalemu; nanyi mpige baragumu[l] katika Tekoa.[m] Na mwinue ishara ya moto katika Beth-hakeremu;[n] kwa sababu msiba umetazama chini kutoka upande wa kaskazini, mshindo mkubwa.[o] **2** Binti Sayuni amefanana kweli na mwanamke mwenye kupendeza na aliye laini.[p] **3** Wachungaji na makundi yao walimjia. Walisimamisha mahema yao pande zote juu yake.[q] Kila mmoja alilisha sehemu yake.[r] **4** Wametakasa vita juu yake:[s] "Simameni, na acheni tupande katikati ya mchana!"[t]

"Ole wetu, kwa maana mchana umepungua, kwa maana vivuli vya jioni vinaendelea kurefuka!"

SURA 5
a Kum 29:4; Yer 4:22
b Isa 59:10
c Isa 6:9; Eze 12:2; Ho 7:11; Mt 13:13; Mk 8:18; Mdo 28:26
d Kum 28:58; Zb 119:120; Ufu 15:4
e Zb 99:1
f Ayu 26:10; Ayu 38:11; Zb 33:7; Zb 104:9; Met 8:29
g Zb 78:8; Zb 81:12; Zb 95:10; Isa 1:23; Isa 65:2; Yer 3:17; Yer 11:8; Yer 18:12; Ho 11:7; Mdo 7:51
h Zb 33:18
i Kum 11:14; Zb 147:8; Yoe 2:23; Yak 5:7
j Mwa 8:22
k Kum 28:23; Zb 107:17; Yer 3:3
l Eze 22:6
m Zb 10:9; Met 1:17; Hab 1:15
n Ho 12:7; Amo 8:5; Mik 6:11

Safu ya 2
a Yer 17:11
b Kum 32:15; Yak 5:5
c Zb 82:2
d Isa 1:23; Zek 7:10
e Ayu 12:6; Zb 73:12; Yer 12:1
f Yer 9:9
g Yer 2:12; Yer 23:14; Ho 6:10
h Yer 14:14; Omb 2:14; Eze 13:6
i Yer 32:32; Mt 27:20
j Isa 30:10; Yoh 3:19; 2Th 2:12; 2Ti 4:3
k Kum 28:29; Isa 10:3

SURA 6
l 2Sa 14:2; 2Nya 11:6; Amo 1:1
m Yer 4:5
n Ne 3:14
o Yer 1:14; Yer 4:6; Yer 10:22
p Isa 3:16
q 2Fa 25:1
r Yer 4:17
s Yoe 3:9
t Yer 15:8

5 "Simameni, twende wakati wa usiku, tukaiharibu minara ya makao yake."[a]

6 Kwa maana Yehova wa majeshi amesema hivi: "Kateni miti[b] na mjenge boma la kuzingira[c] Yerusalemu. Yeye ni jiji ambalo lazima litozwe hesabu.[d] Yeye ni ukandamizaji mtupu katikati yake.[e] **7** Kama tangi linavyoweka maji yake yakiwa baridi, ndivyo yeye alivyouweka ubaya wake ukiwa baridi. Jeuri na uporaji zimesikiwa ndani yake;[f] ugonjwa na tauni ziko mbele za uso wangu sikuzote. **8** Urekebishwe,[g] Ee Yerusalemu, ili nafsi yangu isije ikaondoka kwako ikiwa imechukizwa;[h] ili nisije nikakuweka uwe mahame yenye ukiwa, nchi isiyokaliwa."[i]

9 Yehova wa majeshi amesema hivi: "Bila shaka wataokota mabaki ya Israeli kama mzabibu.[j] Rudisha mkono wako nyuma kama mtu anayekusanya zabibu juu ya vikonyo vya mzabibu."

10 "Nitasema na nani na kumpa nani onyo, ili wasikie? Tazama! Sikio lao halijatahiriwa, hivi kwamba hawawezi kusikiliza.[k] Tazama! Neno la Yehova limekuwa shutuma[l] kwao, na katika neno hilo wao hawawezi kupendezwa.[m] **11** Nami nimejawa na ghadhabu ya Yehova. Nimechoka kujizuia."[n]

"Imwage wakati uleule juu ya mtoto aliye barabarani[o] na juu ya kikundi cha vijana walio rafiki za karibu; kwa maana wao pia watakamatwa, mwanamume pamoja na mke wake, mzee pamoja na mtu mwenye siku nyingi.[p] **12** Na nyumba zao hakika zitapewa wengine ili wazimiliki, na mashamba na wake vilevile.[a] Kwa maana nitanyoosha mkono wangu juu ya wakaaji wa nchi," asema Yehova.[b]

13 "Kwa maana kuanzia aliye mdogo zaidi kati yao mpaka aliye mkubwa zaidi kati yao, kila mmoja anajipatia pato lisilo la haki;[c] na kuanzia nabii mpaka kuhani, kila mmoja anatenda kwa uwongo.[d] **14** Nao wanajaribu kuponya kijuujuu kuvunjika kwa watu wangu,[e] wakisema, 'Kuna amani! Kuna amani!' wakati hakuna amani.[f] **15** Je, waliona aibu kwa sababu jambo walilokuwa wamefanya lilikuwa chukizo?[g] Jambo moja ni kwamba hakika wao hawaoni aibu yoyote; jambo lingine ni kwamba hawajapata kujua hata jinsi ya kufedheheka.[h] Kwa hiyo wataanguka katikati ya wale wanaoanguka;[i] watajikwaa wakati nitakapowatoza hesabu," Yehova amesema.

16 Yehova amesema hivi: "Simameni tuli katika njia, na kuona, na kuuliza juu ya barabara za zamani za kale, mahali ambapo sasa pana njia nzuri;[j] na mtembee ndani yake,[k] na kustarehesha nafsi zenu."[l] Lakini waliendelea kusema: "Hatutatembea."[m] **17** "Nami nilisimamisha walinzi juu yenu,[n] 'Isikilizeni sauti ya baragumu!'"[o] Lakini waliendelea kusema: "Hatutaisikiliza."[p] **18** "Kwa hiyo sikieni, enyi mataifa! Nawe ujue, Ee kusanyiko, jambo litakalokuwa katikati yao. **19** Sikiliza, Ee dunia! Tazama, ninaleta msiba juu ya watu[q] hawa kama matunda ya fikira zao,[r] kwa maana

SURA 6

a 2Nya 36:19
Amo 2:5
b Kum 20:20
c Eze 21:22
Lu 19:43
d Yer 5:9
e 2Fa 21:16
Eze 7:23
f Zb 55:9
Yer 20:8
Eze 7:11
Mik 2:2
g Met 4:13
Sef 3:7
h Eze 23:18
Ho 9:12
i Law 26:34
Yer 2:15
Yer 9:11
j Isa 24:13
Yer 49:9
k Isa 6:10
Yer 7:26
Mdo 7:51
l 2Nya 36:16
Yer 20:8
m 2Ti 4:3
n Yer 20:9
o Yer 9:21
Yer 18:21
p Eze 9:6

Safu ya 2

a Kum 28:30
Yer 8:10
Omb 5:11
Sef 1:13
b Isa 5:25
c Yer 8:10
Eze 22:12
Eze 33:31
Lu 16:14
d Yer 2:8
Yer 14:18
Yer 23:11
Mik 3:5
Mik 3:11
Sef 3:4
e Yer 8:11
f Yer 14:13
Yer 23:17
Eze 13:10
1Th 5:3
g Yer 8:12
Sef 3:5
h Yer 3:3
i Yer 23:12
j Yer 18:15
Mal 4:4
k Isa 2:3
Isa 2:5
Isa 30:21
l Zb 23:3
m Zb 78:10
Isa 42:24
Yer 44:16
n Isa 21:11
Yer 25:4
Eze 3:17
Hab 2:1
o Isa 58:1
p Zek 7:11
q Kum 4:26
Isa 1:2
Da 9:12
r Met 1:31
Isa 59:7

hawakuyasikiliza maneno yangu; na sheria yangu—pia waliendelea kuikataa."[a]

20 "Ina faida gani kwangu kwamba mnaleta ubani kutoka Sheba[b] na kane nzuri kutoka katika nchi ya mbali? Matoleo yenu mazima ya kuteketezwa hayaleti furaha,[c] na dhabihu zenu hazikunipendeza mimi."[d] **21** Kwa hiyo Yehova amesema hivi: "Tazama, ninawawekea watu hawa vikwazo,[e] nao hakika watajikwaa juu yake, akina baba na wana pamoja; jirani na mwenzake—wataangamia."[f]

22 Yehova amesema hivi: "Tazama! Kikundi cha watu kinakuja kutoka nchi ya kaskazini, na kuna taifa kubwa litakaloamshwa kutoka sehemu za mbali zaidi za dunia.[g] **23** Watashika upinde na mkuki.[h] Ni katili, nao hawatakuwa na huruma. Sauti yao itavuma kama bahari,[i] nao watapanda juu ya farasi.[j] Limejipanga katika utaratibu wa vita kama mwanamume wa vita juu yako, Ee binti Sayuni."[k]

24 Tumesikia habari zake. Mikono yetu imelegea.[l] Taabu imetushika, maumivu ya kuzaa kama ya mwanamke anayezaa.[m] **25** Usiende nje shambani, wala usitembee njiani; kwa maana kuna upanga wa adui, kuna woga pande zote.[n] **26** Ee binti ya watu wangu, vaa nguo ya gunia[o] na ugaegae katika majivu.[p] Omboleza kama kumwombolezea mwana wa pekee, kilio cha uchungu;[q] kwa sababu mporaji atakuja juu yetu kwa ghafula.[r]

27 "Nimekufanya wewe kuwa mpimaji wa madini katikati ya watu wangu, mtu anayefanya uchunguzi kamili; nawe utaangalia nawe utaichunguza njia yao.[a] **28** Wote ni watu wakaidi zaidi,[b] wanaotembea wakiwa wachongezi[c]—shaba na chuma. Wote ni wenye kuharibu.[d] **29** Mivukuto[e] imeunguzwa. Risasi inatoka ndani ya moto wao.[f] Mtu ameendelea kusafisha sana kwa ubatili tu, na wale wabaya hawakutengwa.[g] **30** Hakika watu watawaita fedha iliyokataliwa,[h] kwa maana Yehova amewakataa."[i]

7 Neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova, likisema: **2** "Simama katika lango la nyumba ya Yehova, nawe utangaze hapo neno hili,[j] na kusema, 'Sikieni neno la Yehova, ninyi nyote wa Yuda, mnaoingia katika malango haya ili kumwinamia Yehova. **3** Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi: "Fanyeni njia zenu na matendo yenu kuwa mema, nami nitaendelea kuwakalisha mahali hapa.[k] **4** Msiyategemee maneno ya uwongo,[l] mkisema, 'Hekalu la Yehova, hekalu la Yehova, hili ni hekalu la Yehova!' **5** Kwa maana ikiwa hakika mtazifanya njia zenu na matendo yenu kuwa mema, ikiwa hakika mtatenda haki kati ya mtu na mwenzake,[m] **6** ikiwa hamtamkandamiza mkaaji mgeni, mvulana asiye na baba na mjane,[n] nanyi hamtamwaga damu isiyo na hatia mahali hapa,[o] hamtaifuata miungu mingine ili kujiletea wenyewe msiba,[p] **7** mimi, nami, hakika nitaendelea kuwakali-

SURA 6

a Met 28:9
b 1Fa 10:1
Isa 60:6
c Yer 7:21
d Isa 1:11
Isa 66:3
Amo 5:21
e Isa 8:14
f 2Nya 36:17
Isa 9:14
Omb 2:21
g Yer 1:14
Yer 25:9
h Yer 5:16
Yer 50:42
i Yer 10:22
j Hab 1:8
k Yer 4:11
Lu 21:20
l Eze 21:7
m Yer 4:31
Yer 30:6
Yer 49:24
n Yer 4:10
Yer 20:3
o Yer 4:8
p Est 4:3
Yer 25:34
Eze 27:30
Mik 1:10
q Omb 1:2
Omb 1:16
Amo 5:16
Lu 7:12
r Yer 15:8
Yer 48:8

Safu ya 2

a Eze 22:2
Mal 3:2
b Isa 30:1
Isa 48:4
Yer 5:23
Yer 13:10
c 2Sa 19:27
Met 20:19
Yer 9:4
d Isa 1:4
e Eze 22:20
f Yer 9:7
g Eze 24:13
h Isa 1:22
i Yer 14:19
Omb 5:22
Ho 9:17

SURA 7

j Yer 26:2
k Yer 18:11
Yer 26:13
l Mik 3:11
m Yer 21:12
Yer 22:3
n Kum 24:17
Zb 82:3
Zek 7:10
Mal 3:5
Yak 1:27
o Zb 106:38
p Kum 6:14
Kum 8:19
Kum 11:28
Yer 13:10

sha mahali hapa, katika nchi
ambayo niliwapa mababu zenu,
kutoka wakati usio na kipi-
mo mpaka wakati usio na ki-
pimo.'"'"[a]
8 "Tazama, mnayategemea
maneno ya uwongo—hakika
haitakuwa na faida yoyote
kamwe.[b] **9** Je, inawezeka-
na kuwe wizi,[c] uuaji[d] na uzi-
nzi[e] na kuapa kwa uwongo[f]
na kumfukizia Baali moshi[g]
wa dhabihu na kuifuata miungu
mingine ambayo hamku-
ijua,[h] **10** nanyi mje na kusi-
mama mbele zangu katika nyu-
mba hii ambayo jina langu li-
meitwa juu yake,[i] na kusema,
'Hakika tutakombolewa,' huku
mkiyafanya machukizo haya
yote? **11** Je, nyumba hii
ambayo jina langu limeitwa juu
yake,[j] imekuwa pango tu la
wanyang'anyi machoni penu?[k]
Tazama, mimi mwenyewe pia
nimeona jambo hilo," asema
Yehova.[l]
12 "'Hata hivyo, nendeni,
sasa, mahali pangu palipoku-
wa katika Shilo,[m] ambapo nili-
fanya jina langu likae hapo
pale mwanzoni,[n] na kuona ni-
livyopafanya kwa sababu ya
ubaya wa watu wangu Isra-
eli.[o] **13** Na sasa kwa sababu
mliendelea kufanya kazi hizi
zote,' asema Yehova, 'nami ni-
kaendelea kusema nanyi, niki-
amka mapema na kusema,[p]
lakini hamkusikiliza,[q] nami
nikaendelea kuwaita, lakini
hamkujibu,[r] **14** nitaitendea
pia nyumba ambayo jina la-
ngu limeitwa juu yake,[s] amba-
yo mnaitegemea,[t] na mahali
ambapo niliwapa ninyi na ma-
babu zenu, kama nilivyotendea
Shilo.[u] **15** Nami nitawatupa
ninyi nje kutoka mbele za ma-
cho yangu,[a] kama nilivyowatu-
pa nje ndugu zenu wote, uzao
wote wa Efraimu.'[b]
16 "Nawe usisali kwa ajili
ya watu hawa, wala usipaaze
kilio cha kusihi kwa ajili yao
wala sala wala kuniomba,[c] kwa
maana sitakusikiliza.[d] **17** Je,
wewe huoni yale wanayofanya
katika majiji ya Yuda na ka-
tika barabara za Yerusalemu?[e]
18 Wana wanaokota kuni, na
akina baba wanawasha moto,
na wake wanakanda unga ili
kumfanyia 'malkia wa mbingu'
keki za dhabihu;[f] na miungu
mingine inamiminiwa mato-
leo ya kinywaji[g] kusudi wani-
tie uchungu.[h] **19** 'Je, wanani-
tia mimi uchungu?' asema Ye-
hova.[i] 'Je, si wao wenyewe, ku-
sudi watie nyuso zao aibu?'[j]
20 Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amese-
ma hivi, 'Tazama! Hasira ya-
ngu na ghadhabu yangu zina-
mwagwa juu ya mahali hapa,[k]
juu ya mwanadamu na juu ya
mnyama wa kufugwa, na juu
ya mti wa shambani[l] na juu ya
mazao ya udongo; nayo itateke-
teza, wala haitazimwa.'[m]
21 "Yehova wa majeshi, Mu-
ngu wa Israeli, amesema hivi,
'Ongezeni hayo matoleo yenu
mazima ya kuteketezwa kwe-
nye dhabihu zenu na kula nya-
ma.[n] **22** Kwa maana sikuse-
ma na mababu zenu, wala siku-
waamuru wao katika siku nili-
powatoa katika nchi ya Misri,
kuhusu mambo ya toleo
zima la kuteketezwa na dha-
bihu.[o] **23** Lakini niliwaamu-
ru neno hili, nikisema: "Tiini

SURA 7
a Kum 4:40; Yer 3:18
b Isa 30:10; Yer 5:31; Yer 14:14
c Isa 3:14; Eze 22:29; Ho 4:2; Mik 2:2
d Eze 33:25
e Yer 9:2; Mal 3:5
f Yer 5:2
g 1Fa 18:21; 2Fa 23:5; Yer 11:13
h Kut 20:3; Kum 32:17; Amu 5:8
i 2Fa 21:4; 2Nya 33:7; Yer 34:15; Eze 20:39
j Isa 56:7
k Mt 21:13; Mk 11:17; Lu 19:46
l Yer 23:24; Ebr 4:13
m Yos 18:1; Amu 18:31; 1Sa 1:3
n Kum 12:5; Kum 12:11
o 1Sa 4:11; Zb 78:60; Yer 26:6; Yer 26:9
p Yer 25:4
q 2Nya 36:16; Ne 9:29; Yer 11:8; Yer 25:3; Zek 1:4
r Isa 65:12; Isa 66:4; Zek 7:13
s 2Fa 25:9
t Yer 7:4
u 1Sa 4:10; Zb 78:60; Yer 26:6; Omb 2:7

Safu ya 2
a 2Fa 17:23
b 2Nya 25:7; Zb 78:67
c Kut 32:10; Yer 11:14; Yer 14:11
d Isa 1:15; Yer 15:1; Mik 3:4
e Eze 8:6
f Kum 4:19; Kum 17:3; Yer 44:17; Mdo 7:42
g Isa 57:6; Yer 19:13; Eze 20:28
h Isa 3:8; Isa 65:3; Yer 25:7
i Kum 32:16; Eze 8:17; 1Ko 10:22
j Isa 45:16; Yer 20:11; Da 9:7
k Omb 2:3
l Eze 20:47
m 2Fa 22:17; Yer 17:27

n Isa 1:11; Yer 6:20; Ho 8:13; Amo 5:21; o 1Sa 15:22; Zb 51:16; Ho 6:6.

sauti yangu,[a] nami nitakuwa
Mungu wenu,[b] nanyi mtakuwa
watu wangu; na mtembee katika
njia[c] yote ambayo nitawaa-
muru ninyi, ili iwe vema kwe-
nu.”’[d] **24** Lakini hawakusi-
kiliza, wala hawakutega sikio
lao,[e] bali wakatembea katika
mashauri kwa ukaidi wa moyo
wao mbaya,[f] hivi kwamba wa-
kawa watu wa kuelekea nyu-
ma wala si mbele,[g] **25** tangu
siku ile mababu zenu walipoto-
ka katika nchi ya Misri mpaka
leo hii;[h] nami niliendelea ku-
watumia ninyi watumishi wa-
ngu wote manabii, nikiamka
mapema kila siku na kuwatu-
ma.[i] **26** Lakini hawakunisi-
kiliza, nao hawakutega sikio
lao,[j] bali waliendelea kufanya
shingo yao kuwa ngumu.[k] Wa-
litenda vibaya zaidi kuliko ma-
babu zao![l]

27 “Nawe utawaambia mane-
no haya yote,[m] lakini hawataku-
sikiliza; nawe utawaita, lakini
hawatakujibu.[n] **28** Nawe uta-
waambia, ‘Hili ndilo taifa
ambalo watu wake hawakuitii
sauti ya Yehova Mungu wake,[o]
nao hawakushika nidhamu.[p]
Uaminifu umeangamia, nao
umekatiliwa mbali kutoka ka-
tika kinywa chao.’[q]

29 “Nyoa nywele zako
ambazo hazijakatwa na ku-
zitupilia mbali,[r] na kuimba wi-
mbo wa huzuni[s] juu ya vili-
ma vilivyo wazi, kwa maana
Yehova amekikataa[t] naye ata-
kiacha kizazi ambacho ame-
kighadhibikia.[u] **30** ‘Kwa ma-
ana wana wa Yuda wamefa-
nya mambo mabaya machoni
pangu,’ asema Yehova. ‘Wame-
yaweka machukizo yao katika
nyumba ambayo jina langu li-

SURA 7

a Kut 15:26
Law 26:3
Kum 6:3
Yer 11:4
b Kut 19:5
Law 26:12
c Amu 2:22
d Kum 5:29
e Kut 32:8
Ne 9:16
Zb 81:11
Yer 11:8
Eze 20:8
f Kum 29:19
Yer 5:23
Yer 23:17
Eze 3:7
Ho 4:16
Zek 7:12
g Ne 9:26
Isa 1:4
Yer 32:33
h Kum 9:7
1Sa 8:8
Ezr 9:7
i 2Fa 17:13
2Nya 36:15
Ne 9:30
Yer 25:4
j 2Nya 33:10
Yer 11:8
Yer 17:23
Yer 25:3
k 2Fa 17:14
Ne 9:17
Met 29:1
Yer 19:15
Ro 2:5
Ro 10:21
l Yer 16:12
m Yer 26:2
Eze 2:7
Mdo 20:27
n Zek 7:13
o Isa 1:4
Yer 5:4
Sef 3:2
p Zb 50:17
Met 1:7
Sef 3:7
q Yer 5:1
Ho 4:1
Mik 7:2
r Ayu 1:20
Yer 16:6
Mik 1:16
s Eze 19:1
t 2Fa 17:20
u Kum 28:15
Kum 32:20

Safu ya 2

a 2Fa 21:4
2Nya 33:4
Yer 23:11
Yer 32:34
b 2Fa 23:10
2Nya 33:6
Yer 19:6
c Yos 15:8
2Nya 28:3
Yer 19:2
d Kum 12:31
2Fa 17:17
Zb 106:37
Zb 106:38
Isa 57:5
Eze 16:20
Eze 20:31
e Law 18:21
Law 20:3
Kum 17:3
Yer 19:5
Yer 32:35
f Yer 19:6

meitwa juu yake, ili kuitia una-
jisi.[a] **31** Nao wamejenga ma-
hali pa juu pa Tofethi,[b] palipo
katika bonde la mwana wa Hi-
nomu,[c] ili kuwateketeza wana
wao na binti zao katika moto,[d]
jambo ambalo sikuamuru wala
halikuingia moyoni mwangu.’[e]

32 “‘Kwa hiyo, tazama! siku
zinakuja,’ asema Yehova, ‘wa-
kati halitaitwa tena Tofethi na
bonde la mwana wa Hinomu,
bali bonde la uuaji;[f] nao watazi-
ka katika Tofethi bila ya kuwa
na nafasi ya kutosha hapo.[g]
33 Na maiti za watu hawa zi-
takuwa chakula cha viumbe
vinavyoruka vya mbinguni na
cha wanyama wa dunia, pasi-
po mtu yeyote wa kuwatete-
mesha.[h] **34** Nami nitaikome-
sha sauti ya kufurahi na sa-
uti ya kushangilia kutoka ka-
tika majiji ya Yuda na kutoka
katika barabara za Yerusale-
mu sauti ya bwana-arusi na sa-
uti ya bibi-arusi;[i] kwa maana
nchi itakuwa mahali palipofa-
nywa ukiwa.’”[j]

8 “Wakati huo,” asema Yeho-
va, “watu wataleta pia mi-
fupa ya wafalme wa Yuda na
mifupa ya wakuu wake na mi-
fupa ya makuhani na mifu-
pa ya manabii na mifupa ya
wakaaji wa Yerusalemu kutoka
katika makaburi yao.[k] **2** Nao
kwa kweli wataitandaza mbe-
le ya jua na mbele ya mwezi na
mbele ya jeshi lote la mbingu
ambalo wamelipenda na amba-
lo wamelitumikia na ambalo
wamelifuata[l] na ambalo wame-

g 2Fa 23:10; Yer 19:11; Eze 6:5; h Kum 28:26; Zb 79:2; Yer 12:9; Yer 16:4; Yer 34:20; i Isa 24:8; Yer 16:9; Yer 25:10; Eze 26:13; Ho 2:11; j Law 26:33; Isa 1:7; Isa 3:26; Isa 6:11; **SURA 8** k 2Fa 23:16; 2Nya 34:5; Eze 6:5; l Kum 4:19; Kum 17:3; 2Fa 17:16; 2Fa 21:3; Yer 7:9; Yer 19:13; Sef 1:5.

litafuta na ambalo wameliinamia.[a] Haitakusanywa, wala haitazikwa. Itakuwa kama mbolea juu ya uso wa nchi."[b]

3 "Na hakika wale mabaki wa wale wote wanaobaki kutoka katika familia hii mbaya watachagua kifo badala ya uzima[c] katika mahali pote pa wale wanaobaki, ambapo nitakuwa nimewatawanya,"[d] asema Yehova wa majeshi.

4 "Nawe uwaambie, 'Yehova amesema hivi: "Je, wataanguka na wasiamke tena?[e] Mtu akirudi, je, yule mwingine hatarudi pia?[f] **5** Kwa nini watu hawa, Yerusalemu, wanakosa uaminifu kwa ukosefu wa uaminifu unaodumu? Wameshika udanganyifu;[g] wamekataa kurudi.[h] **6** Nimetega sikio,[i] nami niliendelea kusikiliza.[j] Jinsi walivyoendelea kusema haikuwa sawa. Hakuna mtu yeyote aliyekuwa akitubu ubaya wake,[k] akisema, 'Nimefanya nini?' Kila mmoja anarudi katika mwendo unaopendwa na wengi,[l] kama farasi anayekimbia kwenda vitani. **7** Hata korongo juu mbinguni—anajua vema nyakati zake zilizowekwa;[m] na njiwa-tetere[n] na barawai na teleka—huangalia vema wakati wa kila mmoja wao kuingia. Lakini watu wangu hawajaijua hukumu ya Yehova."'[o]

8 "'Ninyi mnawezaje kusema: "Sisi tuna hekima, nasi tuna sheria ya Yehova"?[p] Hakika, sasa, kalamu[q] ya uwongo ya waandishi imefanya kazi ya uwongo mtupu. **9** Wenye hekima wameona aibu.[r] Wameingiwa na woga nao watashikwa. Tazama! Wamelikataa neno la Yehova, nao wana hekima gani?[a] **10** Kwa hiyo nitawapa wanaume wengine wake zao, mashamba yao kwa wale wanaoyamiliki;[b] kwa maana, kuanzia aliye mdogo zaidi mpaka aliye mkubwa zaidi, kila mmoja anajipatia pato lisilo la haki;[c] kuanzia nabii mpaka kuhani, kila mmoja anatenda kwa uwongo.[d] **11** Nao wanajaribu kuponya kijuujuu kuvunjika kwa binti ya watu wangu,[e] wakisema: "Kuna amani! Kuna amani!" wakati hakuna amani.[f] **12** Je, waliona aibu kwa sababu walikuwa wamefanya chukizo?[g] Jambo moja ni kwamba hakika hawakuweza kuona aibu; jambo lingine ni kwamba hawakujua namna ya kufedheheka.[h]

"'Kwa hiyo wataanguka katikati ya wale wanaoanguka. Katika wakati wa kuwakazia fikira,[i] watajikwaa,' Yehova amesema.[j]

13 "'Nitakapokuwa nikikusanya, nitawamaliza,' asema Yehova.[k] 'Hakutakuwa na zabibu juu ya mzabibu,[l] wala hakutakuwa na tini juu ya mtini, na hakika majani yatakauka. Na vitu ninavyowapa vitapita kando yao.'"

14 "Kwa nini tunaketi tuli? Jikusanyeni pamoja, nasi tuingie katika majiji yenye ngome[m] na tunyamaze humo. Kwa maana Yehova Mungu wetu ametunyamazisha,[n] naye anatupa sisi maji yaliyotiwa sumu tunywe,[o] kwa sababu tumemtendea Yehova dhambi. **15** Amani ilitumainiwa, lakini hakuna mema yaliyokuja;[p] wakati wa kuponywa, lakini, tazama! hofu![q] **16** Kukoroma

SURA 8

a 2Fa 23:5 2Nya 33:3 Eze 8:16 Mdo 7:42
b 2Fa 9:37 Zb 83:10 Yer 9:22 Yer 16:4 Yer 25:33
c Ayu 3:21 Ufu 9:6
d Kum 30:1 Yer 29:14 Da 9:7
e Met 24:16 Mik 7:8
f Ho 6:1
g Zb 119:118 Yer 9:6
h Isa 1:20 Yer 5:3
i Ne 9:28
j Zb 14:2 Mal 3:16
k Yer 5:1 2Pe 3:9
l 2Fa 17:15
m Isa 1:3
n Wim 2:12
o Yer 5:4
p Ho 8:12 Ro 2:17
q Isa 8:1
r Isa 29:14

Safu ya 2

a Kum 4:6 Zb 19:7 2Ti 3:15
b Kum 28:30 Yer 6:12 Amo 5:11 Sef 1:13
c Isa 56:11 Yer 6:13 Eze 33:31 Mik 3:11 Tit 1:11
d Yer 5:31 Yer 27:9 Omb 2:14 Omb 4:13 Eze 22:28
e Ayu 13:4 Yer 6:14
f Yer 23:17 Eze 13:10
g Yer 6:15
h Yer 3:3 Flp 3:19
i Isa 10:3 Yer 23:12
j Kum 32:35
k Eze 22:20
l Isa 24:7 Yoe 1:7
m Yer 4:5
n Omb 3:28
o Yer 9:15 Yer 23:15 Omb 3:19
p Yer 4:10 Yer 14:19 Mik 1:12
q Yer 4:15

kwa farasi zake kumesikiwa
kutoka Dani.[a] Kutokana na sa-
uti ya kulia kwa farasi-dume
zake nchi nzima imeanza kuti-
kisika.[b] Nao wanaingia na kui-
la nchi na vyote vilivyomo, jiji
na wakaaji wake."
17 "Kwa maana tazama, ni-
nawatuma nyoka katikati
yenu, nyoka wenye sumu,[c] wa-
sioweza kutumbuizwa,[d] na ha-
kika wao watawauma ninyi,"
asema Yehova.
18 Huzuni isiyoweza kutibi-
wa imeniingia.[e] Moyo wangu ni
mgonjwa. **19** Tazama, kuna
sauti ya kilio cha kuomba msa-
ada cha binti ya watu wangu
kutoka katika nchi ya mbali:[f]
"Je, Yehova hayumo Sayuni?[g]
Au, je, mfalme wake hayumo
ndani yake?"[h]
"Kwa nini wamenitia uchu-
ngu kwa sanamu zao za kucho-
ngwa, kwa miungu yao ya kige-
ni ya ubatili?"[i]
20 "Mavuno yamepita, kia-
ngazi kimeisha; lakini sisi ha-
tukuokolewa!"[j]
21 Nimevunjwa-vunjwa[k]
kwa sababu ya kuvunjika kwa
binti ya watu wangu.[l] Nimehu-
zunika. Mshangao kamili ume-
nishika.[m] **22** Je, hakuna zeri
katika Gileadi?[n] Au, je, ha-
kuna mponyaji humo?[o] Kwa
nini, basi, kupona[p] kwa binti
ya watu wangu hakujatokea?[q]

9 Laiti kichwa changu ki-
ngekuwa maji, na macho
yangu yangekuwa chemche-
mi ya machozi![r] Ndipo ningelia
usiku na mchana kwa ajili ya
waliouawa wa binti ya watu wa-
ngu.[s]
2 Laiti ningekuwa na ma-
hali pa kukaa wasafiri[t] kati-
ka nyika! Ndipo ningewaacha
watu wangu na kwenda mbali
nao, kwa maana wote ni wazi-
nzi,[a] kusanyiko kuu la wanao-
fanya hila;[b] **3** nao wanapinda
ulimi wao uwe upinde wao ka-
tika uwongo;[c] lakini katika ua-
minifu hawajaonyesha kuwa ni
wenye nguvu katika nchi.
endelea kunijia, na kusema:
6 "'Je, mimi siwezi kuwa-
tendea kama mfinyanzi huyu
alivyotenda, enyi nyumba ya

SURA 17
a Zb 25:2
b Yer 18:23
c Yer 16:18
d Ne 8:3
Yer 7:2
e Zb 49:1
Met 1:21
Yer 19:3
Yer 22:2
f Kum 4:9
g Hes 15:32
Ne 13:19
h Kut 20:10
Kut 23:12
Law 23:3
i Kut 31:13
Eze 20:12
j Yer 7:24
Yer 11:10
Eze 20:13
k Met 29:1
Isa 48:4
l Met 1:3
Met 5:12
Sef 3:7
m Kum 11:13
n Yer 17:21
o Kut 34:21
Kum 5:12
p Yer 22:4
q Zb 132:11

Safu ya 2
a Yer 32:44
b Yer 33:13
c Kum 1:7
d Zek 7:7
e Law 1:3
f Ezr 3:3
g Law 2:1
h Law 2:2
i Zb 50:23
Zb 107:22
Zb 116:17
Yer 33:11
Ebr 13:15
j Ne 13:16
k Yer 21:14
Omb 4:11
Amo 1:4
l 2Fa 25:9
2Nya 36:19
Yer 39:8
Yer 52:13
m 2Fa 22:17
Eze 20:47

SURA 18
n Yer 19:1
o Isa 45:9
Ro 9:20

Israeli?' asema Yehova. 'Tazama! Kama udongo mkononi
mwa mfinyanzi, ndivyo ninyi
mlivyo mkononi mwangu, enyi
nyumba ya Israeli.[a] **7** Wakati wowote nikisema juu ya taifa na juu ya ufalme ili kuung'oa na kuubomoa na kuuharibu,[b] **8** na kwa kweli taifa lile ligeuke kutoka katika ubaya wake ambao nilisema juu yake,[c] mimi pia nitajuta juu ya ule msiba niliokuwa nimefikiria kuutimiza juu yake.[d] **9** Lakini wakati wowote ambao huenda nikasema kuhusu taifa na kuhusu ufalme, kuujenga na kuupanda,[e] **10** nao kwa kweli ufanye mabaya machoni pangu kwa kutoitii sauti yangu,[f] mimi pia nitajuta kwa yale mema ambayo nilisema moyoni mwangu kuwa nitafanya kwa faida yake.'

11 "Na sasa, tafadhali, waambie watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu, 'Yehova amesema hivi: "Tazama, ninafanya msiba juu yenu na kutafakari wazo fulani juu yenu.[g] Geukeni, tafadhali, kila mmoja kutoka katika njia yake mbaya, na mfanye njia zenu na matendo yenu kuwa mema."'"[h]

12 Nao wakasema: "Hakuna tumaini![i] Kwa maana sisi tutafuata mawazo yetu wenyewe, nasi tutafanya kila mmoja ukaidi wa moyo wake mbaya."[j]

13 Kwa hiyo Yehova amesema hivi: "Ulizeni wenyewe, tafadhali, kati ya mataifa. Ni nani amesikia mambo kama haya? Kuna jambo lenye kuchukiza sana ambalo bikira wa Israeli amefanya kupita kiasi.[k] **14** Je, theluji ya Lebanoni itatoka katika mwamba wa porini? Au, je, maji mageni, baridi, yanayotiririka, yatakaushwa? **15** Kwa maana watu wangu wamenisahau[a] kwa kuwa wanakifukizia moshi wa dhabihu kitu cha ubatili,[b] na kwa kuwa wanawakwaza watu katika njia zao,[c] mapito ya zamani za kale,[d] kutembea katika barabara, njia ambayo haijatengenezwa ikiwa na mafungu, **16** ili kuifanya nchi yao kuwa kitu cha kushangaza,[e] kuwa ya kupigiwa mluzi mpaka wakati usio na kipimo.[f] Kila mtu anayepita kando yake atatazama kwa mshangao na kutikisa kichwa chake.[g] **17** Nitawatawanya wao mbele ya adui kama kwa upepo wa mashariki.[h] Nitawaonyesha wao mgongo, wala si uso,[i] katika siku ya msiba wao."

18 Nao wakasema: "Njooni, tutafakari juu ya Yeremia wazo fulani,[j] kwa maana sheria haitaangamia kutoka kwa kuhani[k] au shauri kutoka kwa mwenye hekima au neno kutoka kwa nabii.[l] Njooni tumpige kwa ulimi,[m] nasi tusisikilize lolote la maneno yake."

19 Unitegee sikio, Ee Yehova, na kuisikiliza sauti ya wapinzani wangu.[n] **20** Je, ubaya unapaswa kulipwa badala ya wema?[o] Kwa maana wameichimbia nafsi yangu shimo.[p] Ukumbuke kusimama kwangu mbele zako ili kusema mema kuwahusu wao, ili kuigeuza ghadhabu yako iondoke kwao.[q] **21** Kwa hiyo uwatoe wana wao waone njaa,[r] na kuwatoa wapatwe na nguvu za upanga;[s] wake zao na wawe wanawake waliofiwa na watoto, na wajane.[t] Wanaume wao na wauawe

SURA 18

a Ro 9:21
b Yer 1:10
Yer 12:14
Yer 25:9
Yer 45:4
Amo 9:8
Yon 3:4
c 1Fa 8:33
Yer 7:3
Eze 18:21
Eze 33:11
Yon 3:5
d Zb 106:45
Yer 26:3
Yoe 2:13
Yon 3:10
Yon 4:2
e Yer 30:18
Yer 32:41
Amo 9:11
f Zb 125:5
g Yer 26:3
Mik 2:3
h 2Fa 17:13
Isa 1:16
Yer 7:3
Yer 26:13
Eze 18:23
Mdo 26:20
i Yer 2:25
Ro 2:5
Ebr 3:13
j Kum 29:19
Yer 7:24
k Yer 2:13
Yer 5:30

Safu ya 2

a Yer 2:19
Yer 3:21
Yer 13:25
Yer 16:19
Yer 17:13
b Kum 32:21
Isa 41:29
Yer 10:15
c Mal 2:8
d Yer 6:16
e Law 26:33
Yer 19:8
Yer 49:13
Eze 6:14
f Kum 29:24
1Fa 9:8
Omb 2:15
Mik 6:16
g Kum 28:37
Zb 44:14
h Zb 48:7
Yer 13:24
i Kum 31:17
Yer 2:27
j Zb 21:11
Yer 11:19
k Law 10:11
Mal 2:7
l 1Fa 22:24
m Zb 52:2
Met 18:21
n 2Fa 19:16
Ne 4:4
o Zb 109:5
p Zb 35:7
Zb 57:6
Mhu 10:8
q Zb 106:23
Eze 22:30
r Zb 109:10
Yer 11:22
s Yer 12:3
t Kum 32:25
Omb 5:3

kwa tauni yenye kufisha, vijana wao na wapigwe na kuuawa
kwa upanga vitani.[a] **22** Kilio
na kisikiwe kutoka katika nyumba zao, utakapoleta juu yao
kwa ghafula kikundi cha waporaji.[b] Kwa maana wamechimba shimo ili kunikamata, nao
wameficha mitego kwa ajili ya
miguu yangu.[c]

23 Lakini wewe, Ee Yehova,
unajua vema shauri lao lote juu
yangu ili kuniua.[d] Usilifunike
kosa lao, wala usiifute ile dhambi yao kutoka mbele zako;
bali wawe watu waliokwazwa
mbele zako.[e] Katika wakati wa
hasira yako uwachukulie hatua.[f]

19 Yehova amesema hivi:
"Nenda, uchukue chupa ya udongo ya mfinyanzi[g]
na baadhi ya wanaume wa-
zee wa watu na baadhi ya wa-
naume wazee wa makuhani.
2 Nawe uende katika bonde
la mwana wa Hinomu,[h] lililo kwenye mwingilio wa Lango la Vigae. Na hapo utangaze
maneno ambayo nitakuambia.[i]
3 Nawe useme, 'Sikieni neno la
Yehova, enyi wafalme wa Yuda
nanyi wakaaji wa Yerusalemu.[j]
Yehova wa majeshi,[k] Mungu wa
Israeli, amesema hivi:

""Tazama, ninaleta msiba
juu ya mahali hapa, ambao ye-
yote akisikia habari zake, ma-
sikio yake yatawasha;[l] **4** kwa
sababu wameniacha[m] mimi
nao wamepafanya mahali hapa
pasitambuliwe[n] na kufukiza
moshi wa dhabihu ndani yake
kwa miungu mingine amba-
yo hawakuijua,[o] wao pamoja
na mababu zao na wafalme wa
Yuda; nao wamepajaza mahali
hapa damu ya wasio na hatia.[a] **5** Nao walijenga mahali
pa juu pa Baali ili kuwateke-
teza wana wao motoni kama
matoleo mazima ya kuteketezwa kwa Baali,[b] jambo ambalo
sikuliamuru wala kusema juu
yake,[c] na ambalo halikuingia
moyoni mwangu."'[d]

6 ""Kwa hiyo, tazama!
kuna siku zinakuja," asema Ye-
hova, "wakati mahali hapa ha-
pataitwa tena Tofethi[e] na bo-
nde la mwana wa Hinomu,[f] bali
bonde la uuaji. **7** Nami ni-
talivunja shauri la Yuda na la
Yerusalemu mahali hapa,[g]
nami nitawaangusha kwa upa-
nga mbele ya adui zao na kwa
mkono wa wale wanaoitafu-
ta nafsi yao.[h] Na maiti zao ni-
tazitoa ziwe chakula kwa viu-
mbe vinavyoruka vya mbingu-
ni na kwa wanyama wa du-
nia.[i] **8** Nami nitalifanya jiji
hili kuwa kitu cha kushanga-
za na kitu cha kupigiwa mlu-
zi.[j] Kila aliye wa mwisho ata-
kayepita kando yake atatazama
kwa mshangao na kupiga
mluzi kwa sababu ya mapigo
yake yote.[k] **9** Nami nitawa-
fanya wale nyama ya wana wao
na nyama ya binti zao; nao wa-
takula kila mmoja nyama ya
mwenzake, kwa sababu ya ku-
songwa na kwa sababu ya mka-
zo ambao adui zao na wale wa-
naoitafuta nafsi yao watawa-
bania."'[l]

10 "Na uivunje ile chupa
mbele ya macho ya wanaume
wanaoenda pamoja nawe.
11 Nawe uwaambie, 'Yeho-
va wa majeshi amesema hivi:
"Ndivyo nitakavyowavunja
watu hawa na jiji hili kama mtu
anavyokivunja chombo cha
mfinyanzi hivi kwamba haki-

SURA 18
a 2Nya 36:17; Yer 9:21
b Yer 6:26
c Zb 38:12; Zb 64:5; Zb 140:5
d Zb 37:32; Yer 11:19
e Zb 35:4; Zb 59:5; Zb 109:14
f Yer 11:20; Yer 15:15; Ro 2:5

SURA 19
g Yer 18:2; Ro 9:21
h Yos 15:8; 2Fa 23:10; 2Nya 28:3; Yer 7:31
i Met 1:20; Yer 7:2
j Yer 17:20
k Zb 24:10
l 1Sa 3:11; 2Fa 21:12
m Kum 28:20; 2Fa 22:17; Isa 65:11; Yer 2:13; Yer 15:6; Yer 17:13; Da 9:5
n 2Nya 33:4
o Kum 13:6; Kum 32:17; Yer 7:9

Safu ya 2
a 2Fa 21:16; 2Fa 24:4; Isa 59:7; Yer 2:34; Omb 4:13; Mt 23:35; Ufu 16:6
b 2Fa 17:17; 2Nya 28:3; 2Nya 33:6; Zb 106:38; Isa 57:5
c Law 18:21; Yer 32:35
d Yer 7:31
e 2Fa 23:10; Isa 30:33; Yer 7:32
f Yos 15:8
g Met 21:30
h Law 26:17; Kum 28:25
i Kum 28:26; Zb 79:2; Yer 7:33; Yer 16:4; Yer 34:20; Ufu 19:18
j 1Fa 9:8; Yer 18:16; Omb 2:15
k 2Nya 7:21; Yer 25:18
l Law 26:29; Kum 28:53; Isa 9:20; Omb 2:20; Omb 4:10; Eze 5:10

wezi kurekebishwa tena;[a] nao
watazika katika Tofethi[b] mpa-
ka pasiwe na mahali zaidi pa
kuzikia.'"[c]
12 "'Hivyo ndivyo nitaka-
vyopatendea mahali hapa,' ase-
ma Yehova, 'na wakaaji wake,
kulifanya jiji hili kama Tofe-
thi.[d] **13** Na nyumba za Yeru-
salemu na nyumba za wafalme
wa Yuda zitakuwa kama maha-
li pa Tofethi,[e] zitakuwa najisi,
yaani, zile nyumba zote amba-
zo juu ya paa zake walilifukiz-
ia moshi wa dhabihu jeshi lote
la mbinguni[f] na kuimiminia mi-
ungu mingine toleo la kinywa-
ji.'"[g]
14 Kisha Yeremia akatoka
Tofethi,[h] ambapo Yehova aliku-
wa amemtuma ili kutoa unabii,
akasimama katika ua wa
nyumba ya Yehova na kuwaam-
bia watu wote:[i] **15** "Yehova
wa majeshi, Mungu wa Israeli,
amesema hivi, 'Tazama, ninale-
ta juu ya jiji hili na juu ya maji-
ji yake yote msiba wote ambao
nimesema juu yake, kwa sa-
babu wamefanya shingo yao
kuwa ngumu ili wasiyatii ma-
neno yangu.'"[j]

20 Sasa Pashuri mwana wa
Imeri,[k] kuhani, ambaye
pia alikuwa msimamizi mkuu
katika nyumba ya Yehova,[l] akaen-
delea kumsikiliza Yeremia ali-
pokuwa akitoa unabii wa ma-
neno hayo. **2** Ndipo Pashu-
ri akampiga Yeremia nabii[m] na
kumweka katika mikatale[n] ili-
yokuwa katika Lango la Juu
la Benyamini, lililokuwa katika
nyumba ya Yehova. **3** Lakini
ikawa kesho yake kwamba Pa-
shuri akamtoa Yeremia katika
ile mikatale,[o] na sasa Yeremia
akamwambia:

"Yehova amekuita jina lako,[a]
si Pashuri, bali Hofu pande
zote.[b] **4** Kwa maana Yehova
amesema hivi, 'Tazama, nina-
kufanya wewe kuwa hofu kwa-
ko mwenyewe na kwa wapenzi
wako wote, nao hakika wata-
anguka kwa upanga wa adui[c]
zao huku macho yako yaki-
tazama;[d] na Yuda wote nita-
watia mkononi mwa mfalme
wa Babiloni, naye kwa kweli
atawapeleka uhamishoni huko
Babiloni na kuwaua kwa upa-
nga.[e] **5** Nami nitavitoa vitu
vyote vya jiji hili vilivyowe-
kwa akiba na mazao yake yote
na vitu vyake vyote vyenye
thamani; na hazina zote za wa-
falme wa Yuda nitazitia mko-
nono mwa adui zao.[f] Na haki-
ka wao watavipora na kuvichu-
kua na kuvipeleka Babiloni.[g]
6 Na wewe, Ee Pashuri, na wa-
kaaji wote wa nyumba yako,
mtaenda utekwani;[h] nawe uta-
fika Babiloni na huko utakufa
na huko wewe utazikwa pamo-
ja na wapenzi wako wote,[i] kwa
sababu umewatolea unabii wa
uwongo.'"[j]
7 Umenipumbaza, Ee Yeho-
va, hivi kwamba nikapumba-
zika. Ulizitumia nguvu zako
kunipinga mimi, hivi kwa-
mba ukashinda.[k] Nikawa chom-
bo cha kuchekwa mchana
kutwa; kila mtu ananidharau.[l]
8 Kwa maana kila mara nina-
posema, mimi hulia. Jeuri na
uporaji ndizo ninazotangaza.[m]
Kwa maana neno la Yehova
lilikuwa kwangu kisababishi
cha shutuma na cha dhihaka
mchana kutwa.[n] **9** Nami nili-
sema: "Sitamtaja tena, wala si-
tasema tena katika jina lake."[o]

SURA 19
a 2Nya 36:16
Zb 2:9
Isa 30:14
Omb 4:2
Ufu 2:27
b Isa 30:33
Yer 19:6
c Yer 7:32
d 2Fa 23:10
e 2Fa 23:12
2Fa 23:14
Zb 79:1
Eze 7:21
f Yer 8:2
Yer 32:29
Yer 44:17
Sef 1:5
g Yer 7:18
h Yer 19:6
i 2Nya 20:5
2Nya 24:20
Yer 26:2
j Ne 9:17
Ne 9:29
Yer 7:26
Yer 17:23
Zek 7:12
Mdo 7:51

SURA 20
k 1Nya 24:14
l Mdo 5:24
m Mdo 23:2
n 2Nya 16:10
Yer 29:26
Mdo 16:24
o Mdo 4:3

Safu ya 2
a Ho 1:4
b Zb 31:13
Yer 6:25
Yer 46:5
Yer 49:29
Omb 2:22
c Kum 28:65
Zb 73:19
d Kum 28:32
2Fa 25:7
Yer 29:21
Yer 39:6
e Yer 25:9
Yer 39:9
f 2Fa 20:17
2Fa 24:13
2Fa 25:13
Omb 1:10
Eze 22:25
g 2Nya 36:10
Yer 15:13
h Yer 15:2
Yer 29:21
Eze 12:11
i Yer 5:31
j Yer 14:14
Yer 28:15
Yer 29:21
k Eze 3:14
Mik 3:8
l Ayu 12:4
Zb 22:7
Yer 15:10
Omb 3:14
Mdo 17:32
m Yer 6:7
n 2Nya 36:16
Yer 6:10
Yer 15:15
o 1Fa 19:4
Yon 1:3

Na moyoni mwangu hali hiyo
ikawa kama moto unaowaka
ambao umefungiwa ndani ya
mifupa yangu; nami nikachoka kujizuia, nami sikuweza kuivumilia.[a] **10** Kwa maana nilisikia habari mbaya za wengi.[b]
Kulikuwa na hofu pande zote.
"Tangazeni, ili tumtangaze."[c]
Kila mwanadamu anayeweza
kufa anayeniambia "Amani!"
—wanaangalia kuchechemea
kwangu:[d] "Labda atapumbazika,[e] ili tumshinde na tujilipizie
kisasi juu yake." **11** Lakini
Yehova alikuwa pamoja nami[f]
kama mwenye nguvu anayetisha.[g] Ndiyo sababu wale wanaonitesa watajikwaa nao hawatashinda.[h] Hakika watapatwa na aibu kabisa, kwa sababu
hawatakuwa wamefanikiwa.
Fedheha yao inayodumu mpaka wakati usio na kipimo haitasahauliwa.[i]

12 Lakini wewe, Ee Yehova wa majeshi, unamchunguza mwadilifu;[j] unaziona figo na moyo.[k] Na nione kisasi chako
juu yao,[l] kwa maana nimekufunulia wewe kesi yangu.[m]

13 Mwimbieni Yehova! Msifuni Yehova! Kwa maana ameikomboa nafsi ya maskini kutoka mkononi mwa watenda-maovu.[n]

14 Na ilaaniwe ile siku nilipozaliwa! Isibarikiwe ile siku
ambayo mama yangu alinizaa![o] **15** Alaaniwe yule mtu
aliyemletea baba yangu habari njema, akisema: "Amezaliwa kwako mwana, mwanamume!" Hakika yeye alimfanya ashangilie.[p] **16** Na
mtu huyo atakuwa kama majiji ambayo Yehova ameharibu
hali Yeye hakuona majuto yo-

SURA 20

a Ayu 32:18
Zb 39:3
Yer 6:11
Amo 3:8
Mdo 4:20
Mdo 18:5
b Zb 31:13
c Ne 6:6
Met 10:18
Lu 20:20
d Ayu 19:19
Zb 38:16
Zb 41:9
e Lu 11:54
f Isa 41:10
Yer 1:8
Ro 8:31
g Zb 47:2
Zb 66:5
h Kum 32:35
Zb 27:2
Yer 15:15
Yer 15:20
Yer 17:18
i Zb 6:10
Zb 35:26
Zb 40:14
Yer 23:40
j Zb 11:5
Zb 17:3
Yer 17:10
k Zb 7:9
Yer 11:20
l Zb 54:7
Zb 59:10
Yer 17:18
m Zb 62:8
1Pe 2:23
n Zb 35:9
Zb 109:31
o Ayu 3:3
Yer 15:10
p Zb 127:3
Lu 1:58

Safu ya 2

a Mwa 19:25
Kum 29:23
Amo 4:11
2Pe 2:6
b Yer 4:19
Yer 18:22
Sef 1:16
c Ayu 3:10
Ayu 10:18
d Ayu 3:20
Ayu 14:1
e Zb 90:10
Omb 3:1
f Yak 5:10

SURA 21

g Eze 33:30
h 2Fa 24:18
1Nya 3:15
2Nya 36:10
i 1Nya 9:12
Yer 38:1
j 2Fa 25:18
Yer 29:25
Yer 37:3
Yer 52:24
k Amu 20:27
2Fa 22:13
l 2Fa 25:1
Yer 32:28
Yer 39:1
m 1Sa 7:10
2Nya 14:11
Zb 44:1
Zb 105:5
Isa 37:37
n Yer 32:5
Yer 33:5
o Ezr 5:12

yote.[a] Naye atasikia kilio wakati wa asubuhi na king'ora katikati ya mchana.[b]

17 Kwa nini kwa hakika hakuniua ndani ya tumbo la uzazi, ili mama yangu awe kaburi langu na tumbo lake la uzazi liwe na mimba mpaka wakati usio na kipimo?[c] **18** Kwa
nini nimetoka ndani ya tumbo
la uzazi[d] ili kuona kazi ngumu
na huzuni[e] na ili siku zangu zifikie mwisho wake katika aibu tupu?[f]

21 Neno[g] lililomjia Yeremia
kutoka kwa Yehova, wakati Mfalme Sedekia[h] alipotuma kwake Pashuri[i] mwana wa
Malkiya na Sefania[j] mwana wa
Maaseya, kuhani, na kusema:
2 "Tafadhali muulize Yehova[k]
kwa ajili yetu, kwa sababu Nebukadreza mfalme wa Babiloni anapiga vita juu yetu.[l] Labda Yehova atatutendea kulingana na kazi zake zote za ajabu, hivi kwamba yeye aondoke
kwetu."[m]

3 Na Yeremia akawaambia:
"Mwambieni Sedekia hivi,
4 'Yehova Mungu wa Israeli
amesema hivi: "Tazama, ninazigeuza nyuma silaha za vita
zilizo mkononi mwenu, mnazotumia kupigana na mfalme
wa Babiloni,[n] na Wakaldayo[o]
wanaowazingira ninyi nje ya
ukuta, nami nitazikusanya katikati ya jiji hili.[p] **5** Nami nitapigana nanyi[q] kwa mkono
ulionyooshwa na kwa mkono
wenye nguvu na kwa hasira
na kwa ghadhabu na kwa ukali
mkubwa.[r] **6** Nami nitawapiga wakaaji wa jiji hili, mwana-

p Isa 13:4; Eze 16:37; q Isa 63:10; Omb 2:5; r Isa 5:25; Yer 32:17.

damu na mnyama pia. Watakufa kwa tauni kubwa."'[a]

7 ""Na baada ya hayo," asema Yehova, "Nitamtia Sedekia mfalme wa Yuda na watumishi wake na watu na wale wanaobaki katika jiji hili baada ya tauni ile, na upanga na njaa, katika mkono wa Nebukadreza mfalme wa Babiloni, katika mkono wa adui zao na katika mkono wa wale wanaoitafuta nafsi yao, na hakika yeye atawapiga kwa ukali wa upanga na kuwaua.[b] Hatawasikitikia, wala kuwahurumia wala kuwa na rehema yoyote."'[c]

8 "Nawe utawaambia hivi watu hawa, 'Yehova amesema: "Tazama, ninaweka mbele yenu njia ya uzima na njia ya kifo.[d] **9** Yeye anayeketi tuli katika jiji hili atakufa kwa upanga na kwa njaa na kwa tauni;[e] lakini yeye anayetoka nje na ambaye kwa kweli anajitia mkononi mwa Wakaldayo wanaowazingira ninyi ataendelea kuishi, na nafsi yake hakika itakuwa kama nyara kwake."'[f]

10 ""Kwa maana nimekaza uso wangu juu ya jiji hili kwa ajili ya msiba wala si kwa ajili ya mema,"[g] asema Yehova. "Litatiwa mkononi mwa mfalme wa Babiloni,[h] na hakika ataliteketeza kwa moto."[i]

11 "'Na kwa habari ya nyumba ya mfalme wa Yuda, lisikieni neno la Yehova.[j] **12** Enyi nyumba ya Daudi,[k] Yehova amesema hivi: "Kila asubuhi[l] toeni hukumu kwa haki,[m] na kumkomboa kutoka mkononi mwa mpunjaji yeye anayenyang'anywa,[a] ili ghadhabu yangu isitoke kama moto[b] na kuteketeza na kusiwe na yeyote wa kuuzima kwa sababu ya ubaya wa matendo yenu."'[c]

13 "'Tazama, mimi niko dhidi yako, Ee mwanamke mkaaji wa nchi tambarare ya chini,[d] Ee mwamba wa nchi tambarare,' asema Yehova. 'Na kuhusu ninyi ambao mnasema: "Ni nani atakayeshuka kupigana nasi? Na ni nani atakayekuja ndani ya makao yetu?"[e] **14** Mimi pia nitawatoza ninyi[f] hesabu kulingana na matunda ya matendo yenu,'[g] asema Yehova. 'Nami nitawasha moto katika msitu wake,[h] na hakika huo utateketeza vitu vyote vinavyomzunguka.'"[i]

22 Yehova amesema hivi: "Shuka nyumbani kwa mfalme wa Yuda, nawe useme hapo neno hili. **2** Nawe useme, 'Lisikie neno la Yehova, Ee mfalme wa Yuda unayeketi juu ya kiti cha ufalme cha Daudi,[j] wewe pamoja na watumishi wako na watu wako, wale wanaoingia kupitia malango haya.[k] **3** Yehova amesema hivi: "Toeni haki na uadilifu, nanyi mumkomboe yeye anayenyang'anywa kutoka mkononi mwa mpunjaji; wala msimtendee vibaya mkaaji mgeni yeyote, mvulana asiye na baba au mjane.[l] Msiwatendee jeuri yoyote.[m] Wala msimwage damu yoyote isiyo na hatia mahali hapa.[n] **4** Kwa maana mkilifanya neno hili kwelikweli, hakika pia wataingia kupitia malango ya nyumba hii wafalme wanaoketi

SURA 21
a Kum 28:22; Yer 32:24; Eze 7:15
b 2Fa 25:6; 2Nya 36:17; Yer 37:17; Yer 39:5; Yer 52:9; Eze 17:20
c Kum 28:50; 2Nya 36:17; Isa 47:6
d Kum 30:19; Isa 1:19
e Yer 27:13; Yer 38:2; Eze 7:15
f Yer 38:17; Yer 39:18; Yer 45:5
g Law 26:17; Zb 34:16; Yer 44:11; Eze 15:7; Amo 9:4; 1Pe 3:12
h Yer 38:3
i 2Nya 36:19; Yer 17:27; Yer 34:2; Yer 37:10; Yer 39:8; Yer 52:13
j Yer 17:20
k Isa 7:2; Lu 1:69
l Zb 101:8
m 2Sa 8:15; Isa 1:17; Yer 7:5; Yer 22:3; Zek 7:9

Safu ya 2
a Zb 72:4; Met 14:31; Eze 22:29; Mik 2:2
b Kum 32:22; Yer 4:4; Nah 1:6; Sef 1:18
c Isa 1:31; Yer 7:20
d Yer 51:25; Eze 13:8
e 2Sa 5:6; Yer 49:4; Omb 4:12; Oba 3
f Yer 5:9; Yer 9:9
g Met 1:31; Isa 3:11; Ga 6:7
h Isa 10:18
i 2Nya 36:19; Yer 52:13

SURA 22
j Yer 13:13; Yer 17:25; Lu 1:32
k Yer 7:2; Yer 17:20
l Law 19:15; Kum 16:18; Isa 1:17; Yer 21:12; Eze 22:7; Eze 22:29; Mik 2:2; Zek 7:9
m Zb 94:6
n Kum 19:10; 2Fa 24:4; Yer 7:6.

kwa ajili ya Daudi juu ya kiti
chake cha ufalme,[a] wakipanda
magari na farasi, yeye pamo-
ja na watumishi wake na watu
wake."'[b]

5 "'Lakini ikiwa hamtayatii
maneno haya, mimi ninaapa
kwa nafsi yangu mwenyewe,'[c]
asema Yehova, 'kwamba nyu-
mba hii itakuwa ukiwa kabi-
sa.'[d]

6 "Kwa maana Yehova ame-
sema hivi kuhusu nyumba
ya mfalme wa Yuda, 'Wewe ni
kama Gileadi kwangu, kichwa
cha Lebanoni.[e] Hakika nitaku-
fanya uwe nyika;[f] nayo maji-
ji, hakuna hata moja litaka-
lokaliwa.[g] **7** Nami nitataka-
sa juu yako wale wanaoleta
uharibifu,[h] kila mmoja na si-
laha zake;[i] nao wataikata mi-
erezi[j] yako iliyo bora zaidi na
kuiangusha ndani ya moto.[k]
8 Na kwa kweli mataifa me-
ngi watapita kando ya jiji hili
na kila mmoja atamwambia
mwenzake: "Kwa nini Yehova
alilitendea hivi jiji hili kuu?"[l]
9 Nao watasema: "Kwa sababu
wameliacha agano la Yehova
Mungu[m] wao na kuinamia miu-
ngu mingine na kuitumikia."'[n]

10 "Msimlilie aliyekufa,[o]
wala msimsikitikie. Mlilie-
ni sana yule anayeenda zake,
kwa maana hatarudi tena wala
kwa kweli hataiona nchi ya ja-
maa zake. **11** Kwa maana Ye-
hova amesema hivi kumhu-
su Shalumu[p] mwana wa Yo-
sia, mfalme wa Yuda anaye-
tawala badala ya Yosia baba
yake,[q] ambaye ameondoka ma-
hali hapa, 'Hatarudi hapo tena.
12 Kwa maana katika mahali
ambapo wamempeleka uhami-

SURA 22

a 1Fa 2:12
b Yer 17:25
c Hes 23:19
Kum 32:40
Amo 6:8
Ebr 6:17
d Yer 39:8
Mik 3:12
Mal 3:5
e Kum 3:25
f Zb 107:34
Isa 27:10
g Isa 6:11
Isa 24:1
Yer 7:34
h Isa 13:3
i Eze 9:1
j Isa 37:24
k Yer 21:14
Zek 11:1
l 1Fa 9:8
Omb 2:15
m Kum 29:25
Yer 31:32
n Kum 29:26
Kum 31:20
2Fa 22:17
2Nya 34:25
o 2Fa 22:20
p 1Nya 3:15
q 2Fa 23:30
2Nya 36:1

Safu ya 2

a 2Fa 23:34
2Nya 36:4
b 2Fa 23:35
c Law 19:13
Kum 24:14
Mik 3:10
Hab 2:9
Hab 2:12
Mal 3:5
Yak 5:4
d Isa 5:8
e Hag 1:4
f Eze 23:14
g 2Fa 22:2
2Fa 23:25
2Nya 34:2
Met 21:3
Met 31:9
h Kum 4:40
Zb 128:2
Isa 3:10
Yer 42:6
i Ayu 29:12
Zb 72:2
Isa 1:17
j Yos 7:21
Zb 10:3
Zb 119:37
k 2Fa 24:4
l 2Fa 23:34
2Nya 36:4
m 2Sa 1:23
1Fa 13:30
n 1Fa 21:23
Yer 36:30
o 2Nya 36:6

shoni ndipo atakapokufa, naye
hataiona tena nchi hii.'[a]

13 "Ole wake anayejenga
nyumba yake,[b] lakini si kwa
uadilifu, na vyumba vyake vya
juu, lakini si kwa haki, kwa ku-
tumia mwanadamu mwenzake
anayetumikia bure, na ambaye
hampi malipo yake;[c] **14** yeye
anayesema, 'Nitajijengea nyu-
mba yenye nafasi tele na
vyumba vya juu vyenye na-
fasi kubwa;[d] na madirisha ya-
ngu yatapanuliwa kwa ajili
yake, nayo itafunikwa kwa mi-
erezi[e] na kupakwa rangi nye-
kundu.'[f] **15** Je, utaendelea
kutawala kwa sababu unashi-
ndana kwa kutumia mierezi?
Naye baba yako, je, hakula na
kunywa na kutekeleza haki na
uadilifu?[g] Kwa hiyo alifaniki-
wa.[h] **16** Alitetea dai halali la
mwenye kuteseka na maski-
ni.[i] Kwa hiyo akafanikiwa. 'Je,
hiyo haikuwa hivyo kwa sa-
babu ya kunijua mimi?' ase-
ma Yehova. **17** 'Hakika ma-
cho yako na moyo wako havi-
ko juu ya chochote ila pato li-
silo la haki,[j] na juu ya damu
ya asiye na hatia ili kuimwa-
ga,[k] na juu ya kupunja na juu
ya unyang'anyi ili kuyaendele-
za mambo hayo.'

18 "Kwa hiyo Yehova amese-
ma hivi kumhusu Yehoyakimu[l]
mwana wa Yosia, mfalme wa
Yuda, 'Hawataomboleza kwa
ajili yake: "Aa! ndugu yangu!
Na Aa! dada yangu!" Hawataom-
boleza kwa ajili yake: "Aa! Ee
bwana! Na Aa! heshima yake!"'[m]
19 Atazikwa kwa maziko ya
punda-dume,[n] kwa kukokotwa
na kutupwa, nje ya malango ya
Yerusalemu.'[o]

20 "Panda mpaka Lebanoni[a] na upaaze kilio, na juu ya
Bashani[b] upaaze sauti yako.
Na ulie kutoka Abarimu,[c] kwa
sababu wale wote wanaokupenda sana wamevunjwa-vunjwa.[d] **21** Nilisema nawe wakati ulipokuwa huna wasiwasi.[e] Ulisema, 'Sitatii.'[f] Hii
imekuwa njia yako tangu ujana wako, kwa maana hukuitii
sauti yangu.[g] **22** Upepo utawachunga wachungaji wako
wote;[h] na wale wanaokupenda sana wataingia utekwani.[i]
Kwa maana wakati huo utaona aibu na hakika ufedheheke kwa sababu ya msiba wako
wote.[j] **23** Ewe unayekaa katika Lebanoni,[k] unayekaa katika kiota juu ya mierezi,[l] lo! jinsi utakavyougua uchungu wa
kuzaa utakapokujia,[m] uchungu kama wa mwanamke anayezaa!"[n]

24 "'Kama ninavyoishi,'
asema Yehova, 'hata kama Konia[o] mwana wa Yehoyakimu,[p]
mfalme wa Yuda, angekuwa
pete ya muhuri[q] kwenye mkono wangu wa kuume, ningekung'oa wewe kutoka hapo![r]
25 Nami nitakutia wewe katika mkono wa wale wanaoitafuta nafsi yako[s] na katika mkono
wa wale unaoogopa na katika
mkono wa Nebukadreza mfalme wa Babiloni na katika mkono wa Wakaldayo.[t] **26** Nami
nitakutupa wewe pamoja na
mama yako[u] aliyekuzaa mwende katika nchi nyingine
ambayo hamkuzaliwa huko,
nanyi mtakufa huko.[v] **27** Na
katika nchi ambayo watakuwa
wakiiinua nafsi yao ili warudi, hawatarudi huko.[w] **28** Je,
mtu huyu Konia[x] ni umbo tu li-

SURA 22

a Isa 35:2
b Zb 68:15
c Kum 32:49
d 2Fa 24:7
e 2Nya 36:15
f Yer 2:31
Yer 6:16
g Kum 9:7
Amu 2:11
Ne 9:16
Yer 3:25
Yer 7:24
h Yer 23:1
Eze 34:2
Zek 11:8
i 2Fa 24:7
j Yer 2:26
k Yer 22:6
l Isa 2:13
Eze 17:3
m Yer 6:24
Ho 7:14
n Yer 4:31
o 2Fa 24:6
1Nya 3:16
Yer 22:28
Yer 37:1
Mt 1:11
p 2Fa 23:34
q Hag 2:23
r Yer 22:6
s 2Fa 24:15
Yer 21:7
Yer 34:20
t 2Fa 24:11
2Fa 24:16
Ezr 5:12
Met 10:24
Yer 24:1
Yer 27:20
Yer 29:2
u 2Fa 24:12
v 2Fa 24:15
2Nya 36:10
Yer 15:2
w Yer 44:14
Yer 52:34
x Yer 22:24
Yer 37:1

Safu ya 2

a 1Sa 5:4
b Zb 31:12
Yer 48:38
Ho 8:8
c 2Fa 24:15
1Nya 3:17
d Kum 4:26
Kum 32:1
Isa 1:2
Isa 34:1
Yer 6:19
Mik 1:2
e Mt 1:12
f 2Nya 36:10
Yer 36:30
g Lu 1:32

SURA 23

h Yer 10:21
Yer 50:6
Eze 34:2
Zek 11:5
Mt 9:36
i Eze 34:5
j Ho 2:13
Mik 7:4
k Zb 106:47
Isa 11:11
Isa 35:10
Yer 29:14
Yer 31:8
Zek 10:8

lilodharauliwa, lililovunjwa vipande-vipande,[a] au ni chombo
ambacho hakipendezi?[b] Kwa
nini yeye na uzao wake ni lazima waangushwe chini na kutupwa katika nchi ambayo hawakuijua?'[c]

29 "Ee dunia, dunia, dunia,
lisikie neno la Yehova.[d] **30** Yehova amesema hivi, 'Andikeni
kwamba mtu huyu hana mtoto,[e] kama mwanamume ambaye hatafanikiwa kwa vyovyote katika siku zake; kwa maana hakuna hata mmoja atakayefanikiwa kwa vyovyote kutoka
kwa uzao wake,[f] mwenye kuketi juu ya kiti cha ufalme cha
Daudi[g] na kutawala tena katika
Yuda.'"

23 "Ole wao wachungaji
wanaowaangamiza na
kuwatawanya kondoo wa malisho yangu!"[h] asema Yehova.

2 Kwa hiyo Yehova Mungu
wa Israeli amesema hivi juu
ya wachungaji wanaowachunga watu wangu: "Ninyi mmewatawanya kondoo zangu; nanyi mliendelea kuwatawanya,
nanyi hamkuwakazia fikira
zenu."[i]

"Tazama, ninakaza fikira zangu juu yenu kwa sababu ya
ubaya wa matendo yenu,"[j] asema Yehova.

3 "Nami nitakusanya mabaki ya kondoo zangu kutoka katika nchi zote ambako nilikuwa nimewatawanya,[k] nami nitawarudisha kwenye uwanja
wao wa malisho,[l] na hakika
wao watazaa na kuwa wengi.[m]
4 Nami nitasimamisha juu
yao wachungaji ambao kweli

l Kum 30:3; Isa 65:10; Yer 50:19; Eze 34:13; Eze 34:14; Mik 2:12; m Kum 30:5; Amo 9:14.

watawachunga;[a] nao hawataogopa tena, wala hawataingiwa na hofu yoyote,[b] na hakuna hata mmoja atakayekosekana," asema Yehova.

5 "Tazama! Siku zinakuja," asema Yehova, "nami nitamsimamishia Daudi chipukizi adilifu.[c] Na hakika mfalme atatawala[d] na kutenda kwa busara na kutenda haki na uadilifu katika nchi.[e] **6** Katika siku zake Yuda ataokolewa,[f] na Israeli atakaa katika usalama.[g] Na hili ndilo jina lake atakaloitwa, Yehova Ni Uadilifu Wetu."[h]

7 "Kwa hiyo, tazama! siku zinakuja," asema Yehova, "nao hawatasema tena, 'Yehova yuko hai aliyewaleta wana wa Israeli kutoka katika nchi ya Misri,'[i] **8** bali, 'Yehova yuko hai aliyepandisha na aliyeingiza uzao wa nyumba ya Israeli kutoka katika nchi ya kaskazini na kutoka katika nchi zote ambako nimewatawanya,' na hakika wao watakaa katika nchi yao wenyewe."[j]

9 Nao manabii, moyo wangu umevunjika ndani yangu. Mifupa yangu yote imeanza kutetemeka. Nimekuwa kama mtu ambaye amelewa,[k] na kama mwanamume ambaye divai imemlemea, kwa sababu ya Yehova na kwa sababu ya maneno yake matakatifu. **10** Kwa maana nchi imejaa[l] wazinzi.[m] Kwa maana nchi inaomboleza[n] kwa sababu ya laana, viwanja vya malisho vya nyika vimekauka;[o] na mwenendo wao ni mbaya, na nguvu zao si kwa njia ya haki.

11 "Kwa maana nabii pamoja na kuhani wametiwa unajisi.[p] Pia katika nyumba yangu mwenyewe nimeupata ubaya wao,"[a] asema Yehova. **12** "Kwa hiyo njia yao itakuwa kwao kama mahali penye utelezi[b] gizani, ambapo watasukumwa ndani yake na hakika waanguke."[c]

"Kwa maana nitaleta msiba juu yao, mwaka wa kuwakazia fikira,"[d] asema Yehova. **13** "Na katika manabii wa Samaria[e] mimi nimeona jambo lisilofaa. Wametenda kama manabii waliochochewa na Baali,[f] nao wanaendelea kuwafanya watu wangu, Israeli, waende huku na huku.[g] **14** Na katika manabii wa Yerusalemu nimeona mambo yenye kuchukiza sana,[h] kufanya uzinzi[i] na kutembea katika uwongo;[j] nao wameitia nguvu mikono ya watenda-maovu ili wasirudi,[k] kila mmoja kutoka katika ubaya wake. Kwangu wote wamekuwa kama Sodoma,[l] na wakaaji wake kama Gomora."[m]

15 Kwa hiyo Yehova wa majeshi amesema hivi juu ya manabii: "Tazama, ninawalisha pakanga, nami nitawapa maji yaliyotiwa sumu wanywe.[n] Kwa maana kutoka kwa manabii wa Yerusalemu uasi-imani[o] umeenea katika nchi yote."

16 Yehova wa majeshi amesema hivi: "Msiyasikilize maneno ya manabii wanaowatolea ninyi unabii.[p] Wanawafanya muwe ubatili.[q] Wanasema maono ya moyo wao wenyewe[r]—si kutoka katika kinywa cha Yehova.[s] **17** Wanawaambia tena na tena wale ambao hawaniheshimu, 'Ye-

SURA 23

a Yer 3:15
Yoh 21:15
Mdo 20:28
1Pe 5:2
b Mik 5:8
c Isa 4:2
Isa 11:1
Isa 53:2
Yer 33:15
Zek 3:8
Mt 2:23
Yoh 1:45
d Lu 1:32
e Zb 72:2
Isa 9:7
Isa 11:4
Isa 32:1
f 1Fa 4:25
Ho 1:7
Zek 10:6
g Kum 33:28
Zb 130:7
Isa 62:4
Yer 32:37
Zek 14:11
h Isa 54:17
Yer 33:16
i Yer 16:14
j Isa 27:12
Isa 43:5
Eze 34:13
Eze 36:24
Sef 3:20
k Zb 60:3
l Yer 5:7
Eze 22:11
Ho 4:2
m Yer 3:9
Yer 9:2
Yer 13:27
Eze 16:32
Ho 7:4
n Isa 24:4
Yer 12:4
Ho 4:3
Yoe 1:10
o Zb 107:34
Yer 9:10
Yer 12:4
p Isa 28:7
Yer 5:31
Yer 6:13
Yer 8:10
Eze 22:25
Sef 3:4

Safu ya 2

a 2Nya 33:5
2Nya 36:14
Yer 7:11
Eze 8:11
Eze 23:39
b Zb 35:6
Zb 73:18
Met 4:19
Yer 13:16
c Kum 28:15
d Yer 8:12
Yer 11:23
e Eze 16:46
f Yer 2:8
g 2Nya 33:9
Isa 9:16
h Yer 18:13
i Yer 29:23
j Yer 14:14
Yer 23:26
k Kum 30:10
Mal 3:7
l Isa 3:9
m Mwa 18:20
Kum 32:32
Isa 1:10
Yud 7
n Yer 8:14
Yer 9:15

o Met 11:9; Isa 9:17; Isa 24:5; p Yer 27:9; Yer 29:8; q 2Fa 17:15; Yer 2:5; r Omb 2:14; s Yer 14:14; Yer 28:15; Eze 13:3; Eze 22:28.

hova amesema: “Ninyi mtakuwa na amani.”’[a] Nao wamemwambia kila mtu anayetembea katika ukaidi wa moyo wake,[b] ‘Hamtapatwa na msiba wowote.’[c] **18** Kwa maana ni nani amesimama katika kikundi cha rafiki[d] za Yehova ili aone na kulisikia neno lake?[e] Ni nani amelikazia fikira neno lake ili alisikie?[f] **19** Tazama! Dhoruba ya Yehova, ghadhabu, hakika itatoka, tufani inayozunguka.[g] Itajizungusha juu ya kichwa cha waovu.[h] **20** Hasira ya Yehova haitarudi nyuma mpaka atakapokuwa ametenda[i] na mpaka atakapokuwa ametimiza mawazo ya moyo wake.[j] Katika siku za mwisho ninyi mtalifikiria jambo hilo kwa uelewaji.[k]

21 “Sikuwatuma manabii, ingawa wao wenyewe walikimbia. Sikusema nao, ingawa wao wenyewe walitoa unabii.[l] **22** Lakini ikiwa wangekuwa wamesimama katika kikundi changu cha rafiki,[m] ndipo wangewafanya watu wangu wayasikie maneno yangu, nao wangewarudisha kutoka katika njia yao mbaya na kutoka katika ubaya wa matendo yao.”[n]

23 “Je, mimi ni Mungu aliye karibu,” asema Yehova, “na si Mungu aliye mbali?”[o]

24 “Au, je, mtu yeyote anaweza kujificha katika maficho nami nisimwone?”[p] asema Yehova.

“Je, mimi kwa kweli sizijazi mbingu na dunia?”[q] asema Yehova. **25** “Nimesikia yale ambayo manabii wanaotoa unabii wa uwongo katika jina langu[r] wamesema, ‘Nimeota ndoto! Nimeota ndoto!’[a] **26** Itadumu mpaka wakati gani katika moyo wa manabii wanaotoa unabii wa uwongo na ambao ni manabii wa udanganyifu wa moyo wao wenyewe?[b] **27** Wanafikiria kuwafanya watu wangu walisahau jina langu kwa njia ya ndoto zao ambazo wanaendelea kusimuliana,[c] kama baba zao walivyolisahau jina langu kwa sababu ya Baali.[d] **28** Nabii ambaye ana ndoto, na asimulie ndoto hiyo; lakini yule ambaye ana neno langu, na aliseme neno langu kwa ukweli.”[e]

“Nyasi ina uhusiano gani na nafaka?”[f] asema Yehova.

29 “Je, neno langu halilinganani na moto,”[g] asema Yehova, “na kama nyundo ya chuma ambayo huvunja mwamba?”[h]

30 “Kwa hiyo tazama, mimi niko dhidi ya manabii,”[i] asema Yehova, “wale wanaoyaiba maneno yangu, kila mmoja kutoka kwa mwenzake.”[j]

31 “Tazama, mimi niko dhidi ya manabii,” asema Yehova, “wale wanaotumia ulimi wao ili kusema, ‘Neno!’”[k]

32 “Tazama, mimi niko dhidi ya manabii wa ndoto za uwongo,” asema Yehova, “wale wanaozisimulia na kuwafanya watu wangu kwenda huku na huku kwa sababu ya uwongo[l] wao na kwa sababu ya kujisifu[m] kwao.”

“Lakini mimi mwenyewe sikuwatuma wala kuwaamuru. Kwa hiyo hawatawafaidi watu hawa kwa vyovyote,”[n] asema Yehova.

33 “Na watu hawa au nabii au kuhani wanapokuuliza, wakisema, ‘Mzigo wa Yehova ni nini?’[o]

SURA 23

a Yer 4:10
Yer 6:14
Yer 8:11
Eze 13:10
b Kum 29:19
Yer 3:17
c Amo 9:10
Mik 3:11
d Zb 25:14
Zb 89:7
Yer 23:22
e Amo 3:7
f 2Nya 33:10
g Isa 5:25
Yer 25:32
h Amu 9:57
1Sa 25:39
Ne 4:4
Yer 30:23
Yoe 3:7
Oba 15
i Law 26:28
Zek 8:14
j Yer 30:24
k 1Fa 8:47
l Yer 14:14
Yer 27:15
Yer 29:9
m Ayu 29:4
Zb 15:1
Zb 25:14
Yer 23:18
n Yer 25:5
Yer 29:23
o Zb 113:6
Mdo 17:27
p Mwa 16:13
Zb 90:8
Zb 139:7
Met 15:3
Amo 9:2
Ebr 4:13
q Zb 139:7
Isa 66:1
r Yer 29:23

Safu ya 2

a Kum 13:1
Kum 18:20
Yer 27:9
Zek 10:2
b Yer 14:14
Yer 17:9
c Kum 13:2
Mdo 13:8
d Amu 3:7
2Fa 21:3
e Met 14:5
Lu 12:42
2Ko 2:17
f Isa 41:16
Lu 3:17
1Ko 3:13
g Isa 30:27
Yer 5:14
Yer 20:9
h Ebr 4:12
i Kum 18:20
Yer 14:15
Eze 13:2
Mt 24:24
j 2Sa 15:6
Zb 50:17
k Eze 13:7
l Kum 13:1
Kum 18:20
Zek 10:2
m Sef 3:4
n Yer 7:8
Omb 2:14
Mt 15:14
o Yer 17:15
Hab 1:1
Mal 1:1

wewe pia utawaambia, ‘“Ninyi
—Lo! jinsi mlivyo mzigo![a] Nami
nitawaacha ninyi,”[b] asema
Yehova.’ **34** Naye nabii au ku-
hani au watu wanaosema, ‘Mzi-
go wa Yehova!’ Mimi pia nitaka-
za fikira zangu juu ya mtu
huyo na juu ya nyumba yake.[c]
35 Hivi ndivyo mnavyoendelea
kuambiana mtu na mwenzake
na mtu na ndugu yake, ‘Yeho-
va ametoa jibu gani? Na Yeho-
va amesema nini?’[d] **36** Lakini
msiutaje tena[e] mzigo[f] wa Yeho-
va, kwa maana kwa kila mmo-
ja mzigo unakuwa ni neno lake
mwenyewe,[g] nanyi mmeyaba-
dili maneno ya Mungu aliye
hai,[h] Yehova wa majeshi, Mungu
wetu.

37 “Utamwambia huyo na-
bii hivi, ‘Yehova amekupa
jibu gani? Na Yehova amesema
nini?[i] **38** Na ikiwa mnaende-
lea kusema, “Mzigo wa Yeho-
va!” basi Yehova amesema hivi:
“Kwa sababu mnasema, ‘Hili
neno ndilo mzigo wa Yehova,’
nilipoendelea kumtuma mtu
kwenu, na kusema, ‘Msiseme:
“Mzigo wa Yehova!”’ **39** kwa
hiyo mimi hapa! Nami nitawa-
puuza ninyi, kabisa,[j] nami ni-
tawatupa pamoja na lile jiji
nililowapa ninyi na mababu
zenu—kutoka mbele zangu.[k]
40 Nami nitatia juu yenu shu-
tuma mpaka wakati usio na ki-
pimo na fedheha mpaka waka-
ti usio na kipimo, ambayo hai-
tasahauliwa.”’”[l]

24 Na Yehova akanionye-
sha, na, tazama! vikapu
viwili vya tini vilivyowekwa
mbele ya hekalu la Yehova, ba-
ada ya Nebukadreza mfalme
wa Babiloni kumpeleka uhami-
shoni Yekonia[a] mwana wa Ye-
hoyakimu,[b] mfalme wa Yuda,
na wakuu wa Yuda na mafu-
ndi[c] na wajenzi wa maboma,
kutoka Yerusalemu ili awale-
te Babiloni.[d] **2** Nacho kika-
pu kimoja, tini zilikuwa nzu-
ri sana, kama tini za mapema;[e]
nacho kile kikapu cha pili, tini
zilikuwa mbaya sana, hivi kwa-
mba hazingeweza kuliwa kwa
sababu ya ubaya.

3 Kisha Yehova akaniambia:
“Unaona nini, Yeremia?” Basi
nikasema: “Tini, zile tini nzu-
ri zikiwa nzuri sana, na zile
mbaya zikiwa mbaya sana, hivi
kwamba haziwezi kuliwa kwa
sababu ya ubaya.”[f]

4 Ndipo neno la Yehova li-
kanijia, na kusema: **5** “Yeho-
va Mungu wa Israeli amesema
hivi, ‘Kama hizi tini nzuri, ndi-
vyo nitakavyowaona kwa
njia nzuri[g] wale wahamishwa
wa Yuda, ambao nitawapele-
ka kutoka mahali hapa mpa-
ka katika nchi ya Wakaldayo.[h]
6 Nami nitaweka jicho langu
juu yao kwa njia nzuri,[i] na
hakika mimi nitawarudisha
katika nchi hii.[j] Nami nita-
wajenga, wala sitawabomoa;
nami nitawapanda, wala si-
tawang’oa.[k] **7** Nami nitawa-
pa moyo wa kunijua,[l] kwamba
mimi ni Yehova; nao watuku-
wa watu wangu,[m] nami nitaku-
wa Mungu wao, kwa maana wa-
tarudi kwangu kwa moyo wao
wote.[n]

8 “‘Na kama zile tini mbaya
ambazo haziwezi kuliwa kwa
sababu ya ubaya,[o] kwa kweli
Yehova amesema hivi: “Ndivyo
nitakavyomtoa Sedekia[p] mfa-
lme wa Yuda na wakuu wake
na mabaki wa Yerusalemu wa-

SURA 23
a Hes 11:14
b Kum 31:17; Yer 12:7; Ho 9:12
c Mik 7:4
d Yer 31:34; Ebr 8:11
e Ne 13:18
f Kut 19:8; 1Nya 9:33
g Amu 17:6
h Yer 2:21; Yer 2:36
i Eze 18:25
j Kum 31:17; Ho 4:6
k Yer 23:33; Omb 5:20
l Yer 20:11; Yer 24:9; Yer 42:18; Da 9:16

Safu ya 2

SURA 24
a 2Fa 24:12; Est 2:6; Eze 19:9
b 2Fa 24:6; 1Nya 3:16; Yer 22:24
c 2Fa 24:16
d Yer 29:2
e Isa 28:4; Ho 9:10
f Yer 24:8
g Yer 29:10
h Yer 25:11
i 2Nya 16:9; 1Pe 3:12
j Ezr 1:3; Yer 12:15; Yer 23:3; Yer 29:10; Eze 36:24
k Yer 1:10; Yer 30:18; Yer 32:41; Yer 33:7
l Kum 30:6; Yer 31:33; Eze 11:19
m Yer 30:22; Yer 32:38; Eze 14:11; Zek 8:8; Ebr 8:10
n 1Fa 8:48; Yer 29:13
o Yer 29:17
p 2Fa 25:7; Eze 12:13

naobaki katika nchi hii[a] na
wale wanaokaa katika nchi ya
Misri[b]— **9** mimi pia nitawa-
toa kwa ajili ya kutetemesha,
kwa ajili ya msiba, katika fa-
lme zote za dunia,[c] kwa aji-
li ya shutuma na kwa ajili ya
neno la kimethali, kwa ajili ya
suto[d] na kwa ajili ya laana,[e]
katika mahali pote nitakapo-
watawanya.[f] **10** Nami nitatu-
ma juu yao upanga,[g] njaa[h] na
tauni,[i] mpaka waufikie mwisho
wao kutoka katika nchi niliyo-
wapa wao na mababu zao.'"'[j]

25 Neno lililomjia Yeremia
kuhusu watu wote wa
Yuda katika mwaka wa nne
wa Yehoyakimu[k] mwana wa Yo-
sia, mfalme wa Yuda, yaani,
mwaka wa kwanza wa Nebu-
kadreza mfalme wa Babiloni;
2 ambalo Yeremia nabii alise-
ma kuhusu watu wote wa Yuda
na kuhusu wakaaji wote wa Ye-
rusalemu, akisema:

3 "Tangu mwaka wa 13 wa
Yosia[l] mwana wa Amoni, mfa-
lme wa Yuda, mpaka leo hii,
miaka hii 23, neno la Yeho-
va limenijia, nikaendelea ku-
sema nanyi, nikiamka mape-
ma na kusema, lakini hamkusi-
kiliza.[m] **4** Na Yehova alituma
kwenu watumishi wake wote
manabii, akiamka mapema na
kuwatuma, lakini hamkusikili-
za,[n] wala hamkutega sikio lenu
ili kusikiliza,[o] **5** wao wakise-
ma, 'Tafadhali, geukeni kila
mmoja kutoka katika njia yake
mbaya na kutoka katika uba-
ya wa matendo yake,[p] nanyi
mwendelee kukaa juu ya nchi
ambayo Yehova aliwapa ninyi
na mababu zenu tangu zama-
ni za kale na mpaka wakati
mrefu ujao.[a] **6** Nanyi msifu-
ate miungu mingine ili kuitu-
mikia na kuiinamia, ili msini-
tie uchungu mimi kwa kazi ya
mikono yenu, na ili nisiwaletee
ninyi msiba.'[b]

7 "'Lakini hamkunisikiliza
mimi,' asema Yehova, 'kusudi
mnitie uchungu kwa kazi ya
mikono yenu, ili kujiletea we-
nyewe msiba.'[c]

8 "Kwa hiyo Yehova wa ma-
jeshi amesema hivi, '"Kwa sa-
babu hamkuyatii maneno ya-
ngu, **9** tazama, ninatuma,
nami nitazichukua familia
zote za kaskazini,"[d] asema Ye-
hova, "nitatuma ujumbe kwa
Nebukadreza mfalme wa Babi-
loni, mtumishi wangu,[e] nami
nitawaleta wao juu ya nchi hii[f]
na juu ya wakaaji wake na juu
ya haya mataifa yote kuzungu-
ka pande zote;[g] nami nitawa-
angamiza na kuwafanya kuwa
kitu cha kushangaza na kitu
cha kupigiwa mluzi[h] na ukiwa
mpaka wakati usio na kipimo.[i]
10 Nami nitaangamiza kuto-
ka ndani yao sauti ya furaha
na sauti ya shangwe,[j] sauti ya
bwana-arusi na sauti ya bibi-
arusi,[k] sauti ya jiwe la kusa-
gia la mkononi[l] na nuru ya
taa.[m] **11** Na nchi hii yote ita-
kuwa mahali palipoharibiwa,
kitu cha kushangaza, na mata-
ifa haya yatamtumikia mfalme
wa Babiloni miaka 70."'[n]

12 "'Na itatukia kwamba
miaka 70 itakapotimia[o] nitato-
za hesabu juu ya mfalme wa
Babiloni na juu ya taifa lake,'[p]
asema Yehova, 'kwa sababu
ya kosa lao, juu ya nchi ya

SURA 24

a Law 26:39
b Yer 43:7
Yer 44:1
Yer 46:13
c Yer 15:4
Yer 34:17
d Kum 28:37
1Fa 9:7
2Nya 7:20
Zb 44:13
e Kum 28:15
Kum 29:27
Yer 26:6
Yer 29:22
f Kum 28:64
Yer 29:18
g Law 26:33
Yer 9:16
h Yer 14:15
Yer 15:2
i Kum 28:59
Eze 7:15
j Kum 28:63

SURA 25

k 2Fa 24:1
Yer 36:1
Yer 46:2
Da 1:1
l Yer 1:2
m 2Nya 36:15
Zb 81:13
Yer 7:13
Yer 11:7
Yer 13:10
Yer 16:12
n Yer 7:13
Yer 29:19
Yer 44:4
o Zek 7:11
Mdo 7:51
p 2Fa 17:13
Isa 55:7
Yer 18:11
Yer 35:15
Eze 18:30
Eze 33:11
Yon 3:8
Zek 1:4
Mal 3:7
2Pe 3:9

Safu ya 2

a Zb 105:11
b Kut 20:5
Kum 6:15
Yos 24:20
c Kum 32:21
2Fa 17:17
Ne 9:26
Yer 7:19
Yer 32:30
Yer 44:5
d Law 26:25
Isa 5:26
Yer 1:15
Yer 5:15
e Yer 27:6
Yer 43:10
Eze 29:18
f Kum 28:49
Yer 5:15
Eze 7:24
Amo 6:14
g Eze 26:7
Eze 29:19
Hab 1:6
h Yer 19:8
i 1Fa 9:7
Yer 18:16
j Isa 24:7
Eze 26:13
k Yer 7:34
Yer 16:9
l Ufu 18:22

m Ufu 18:23; n 2Nya 36:21; Da 9:2; Zek 1:12; Zek 7:5; o Kum 30:3; Ezr 1:1; Yer 29:10; p Isa 13:1; Isa 14:4; Isa 47:1; Yer 51:1; Da 5:26; Da 5:30.

Wakaldayo,[a] nami nitaifanya
kuwa mahame yenye ukiwa
mpaka wakati usio na kipimo.[b]
13 Nami nitaleta juu ya nchi
ile maneno yangu yote ambayo
nimesema juu yake, yote amba-
yo yameandikwa katika kita-
bu hiki ambacho Yeremia ame-
toa unabii juu ya mataifa yote.[c]
14 Kwa maana hata wao we-
nyewe, mataifa mengi na wafa-
lme wakubwa,[d] wamewatumia
vibaya kama watumishi;[e] nami
nitawalipa kulingana na mate-
ndo yao na kulingana na kazi
ya mikono yao.'"[f]

15 Kwa maana Yehova Mu-
ngu wa Israeli ameniambia
hivi: "Chukua kikombe hiki
cha divai ya ghadhabu kutoka
mkononi mwangu, nawe uki-
nyweshe[g] mataifa yote ambayo
ninakutuma kwao. **16** Nao
lazima wanywe na kuyumba-
yumba na kutenda kama we-
nda-wazimu kwa sababu ya
upanga ninaotuma katikati
yao."[h]

17 Ndipo nikakichukua kile
kikombe kutoka mkononi mwa
Yehova na kukinywesha mata-
ifa yote ambayo Yehova aliku-
wa amenituma kwao:[i] **18** ya-
ani, Yerusalemu na majiji ya
Yuda na wafalme wake, wakuu
wake, ili kuyafanya kuwa ukiwa,
kitu cha kushangaza,[j] kitu
cha kupigiwa mluzi na laana,
kama ilivyo leo hii;[k] **19** Fa-
rao mfalme wa Misri na wa-
tumishi wake na wakuu wake
na watu wake wote;[l] **20** na
jamii yote iliyochangamana,
na wafalme wote wa nchi ya
Usi,[m] na wafalme wote wa nchi
ya Wafilisti[n] na Ashkeloni[o] na
Gaza[p] na Ekroni[q] na maba-
ki ya Ashdodi;[r] **21** Edomu[s]
na Moabu[a] na wana wa Amoni;[b]
22 na wafalme wote wa Tiro[c]
na wafalme wote wa Sidoni[d]
na wafalme wa kisiwa kilicho
katika eneo la bahari; **23** na
Dedani[e] na Tema[f] na Buzi na
wale wote wenye nywele zilizo-
katwa kwenye vipaji vya nyu-
so;[g] **24** na wafalme wote wa
Waarabu[h] na wafalme wote
wa jamii iliyochangamana wa-
naokaa nyikani; **25** na wafa-
lme wote wa Zimri na wafalme
wote wa Elamu[i] na wafalme
wote wa Wamedi;[j] **26** na wa-
falme wote wa kaskazini wa-
lio karibu na walio mbali, mmo-
ja baada ya mwingine, na falme
nyingine zote za dunia zilizo
juu ya uso wa nchi; naye mfa-
lme wa Sheshaki[k] atakunywa
baada yao.

27 "Nawe utawaambia, 'Ye-
hova wa majeshi, Mungu wa
Israeli, amesema hivi: "Ku-
nyweni, mlewe, mtapike na
kuanguka hivi kwamba msi-
weze kusimama[l] kwa sababu
ya upanga ninaotuma katikati
yenu."'[m] **28** Na iwe kwamba
wakikataa kukichukua kiko-
mbe kutoka mkononi mwako
ili wanywe, wewe pia utawaa-
mbia, 'Yehova wa majeshi ame-
sema hivi: "Bila shaka mta-
kinywa.[n] **29** Kwa maana, ta-
zama! ninaanza kuleta msi-
ba[o] juu ya jiji ambalo linaitwa
kwa jina langu, nanyi, je, mna-
paswa kwa vyovyote kuachwa
bila kuadhibiwa?"'[p]

"'Hamtaachwa bila kuadhi-
biwa, kwa maana kuna upanga
ambao ninaita juu ya wakaaji
wote wa dunia,' asema Yehova
wa majeshi.

SURA 25

a 2Fa 24:1
b Isa 13:19
Isa 14:23
c Yer 1:5
Yer 1:10
d Yer 50:9
Yer 51:27
e Isa 14:2
Yer 50:41
Yer 51:7
Hab 2:8
f Zb 137:8
Yer 50:29
Yer 51:6
Yer 51:24
Ufu 18:6
g Ayu 21:20
Zb 75:8
Isa 51:17
Yer 25:26
Ufu 14:10
Ufu 16:19
h Yer 51:7
Omb 4:21
Eze 23:34
Nah 3:11
i Yer 1:10
Yer 27:3
Yer 51:7
j 2Fa 22:19
Yer 24:9
k Ezr 9:7
Yer 44:22
l Yer 46:2
Eze 29:2
Eze 32:31
m Ayu 1:1
n Isa 14:31
Yer 47:1
Eze 25:15
Amo 1:8
Sef 2:5
Zek 9:6
o Yer 47:5
Sef 2:4
p Yos 13:3
q Zek 9:5
r Isa 20:1
s Isa 34:5
Yer 49:17
Eze 35:15

Safu ya 2

a Yer 48:1
Eze 25:8
b Yer 49:1
Eze 25:2
Amo 1:13
c Isa 23:15
Eze 28:2
d Yer 27:3
Yer 47:4
Eze 32:30
e Isa 21:13
Yer 49:8
Eze 25:13
f Isa 21:14
g Yer 9:26
Yer 49:32
h 2Nya 9:14
Yer 49:31
i Yer 49:34
Eze 32:24
j Yer 51:11
k Yer 51:41
l Isa 63:6
Omb 4:21
Hab 2:16
m Eze 21:4
n Zb 75:8
o 1Fa 9:7
Yer 7:14
Da 9:18
1Pe 4:17
p Met 11:31; Yer 49:12; Oba 16.

30 “Nawe utawatolea unabii
kwa maneno haya yote, nawe
utawaambia, ‘Yehova atanguruma kutoka juu,[a] naye atatoa
sauti yake kutoka katika makao yake matakatifu.[b] Bila shaka atanguruma juu ya makao
yake. Atapaaza sauti kama ile
ya wale wanaokanyaga shinikizo la divai juu ya wakaaji wote
wa dunia.’[c]
31 “‘Hakika kelele zitafika
mpaka sehemu ya mbali zaidi ya dunia, kwa maana Yehova ana ubishi na mataifa.[d] Yeye
binafsi atajiweka hukumuni na
watu wote wenye mwili.[e] Nao
waovu atawatoa wauawe kwa
upanga,’[f] asema Yehova.
32 “Yehova wa majeshi amesema hivi, ‘Tazama! Msiba utaenda toka taifa mpaka taifa,[g]
na tufani kuu itaamshwa kutoka katika sehemu za mbali zaidi za dunia.[h] **33** Na wale wa-
liouawa na Yehova siku hiyo
hakika watakuwa kutoka mwisho mmoja wa dunia mpaka
mwisho wa pili wa dunia.[i] Hawataombolezewa, wala kukusanywa wala kuzikwa.[j] Watakuwa kama mbolea juu ya uso
wa nchi.’[k]
34 “Pigeni mayowe, ninyi
wachungaji, na mpaaze kilio![l]
Na mgaegae,[m] ninyi watu mashuhuri wa kundi,[n] kwa sababu siku za kuchinjwa kwenu na za kutawanywa kwenu
zimetimia,[o] nanyi mtaanguka
kama chombo kinachotamanika![p] **35** Na makimbilio yameangamia kwa wachungaji, na
njia ya kuponyoka kwa watu
mashuhuri wa kundi.[q] **36** Sikilizeni! Kilio cha wachungaji,
na kupiga mayowe kwa watu
mashuhuri wa kundi, kwa
maana Yehova anapora malisho yao. **37** Na makao yenye
amani yamefanywa kukosa
uhai kwa sababu ya hasira ya
Yehova inayowaka.[a] **38** Ametoka katika maficho yake kama
mwana-simba mwenye manyoya shingoni,[b] kwa maana nchi
yao imekuwa kitu cha kushangaza kwa sababu ya upanga
unaoonea na kwa sababu ya
hasira yake inayowaka.”[c]

26 Katika mwanzo wa utawala wa kifalme wa Yehoyakimu[d] mwana wa Yosia,
mfalme wa Yuda, neno hili lilikuja kutoka kwa Yehova, na
kusema: **2** “Yehova amesema hivi, ‘Simama katika ua wa
nyumba ya Yehova,[e] nawe useme kuhusu majiji yote ya Yuda
yanayokuja kuinama katika
nyumba ya Yehova, useme maneno yote nitakayokuamuru uwaambie.[f] Usiondoe hata
neno moja.[g] **3** Labda watasikiliza na kurudi, kila mmoja
kutoka katika njia yake mbaya,[h] nami nitajuta msiba ninaofikiria kuleta juu yao kwa sababu ya ubaya wa matendo yao.[i]
4 Nawe uwaambie: “Yehova
amesema hivi, ‘Ikiwa hamtanisikiliza kwa kutembea katika sheria yangu[j] ambayo nimeweka mbele yenu,[k] **5** kwa
kuyasikiliza maneno ya watumishi wangu manabii, ambao
ninawatuma kwenu, nikiamka
mapema na kuwatuma, ambao
hamkuwasikiliza,[l] **6** mimi,
kwa upande wangu, nitaifanya
nyumba hii kama ile iliyo katika Shilo,[m] na jiji hili nitalifanya kuwa laana kwa mataifa
yote ya dunia.’””[n]

SURA 25
a Isa 42:13; Yoe 3:16; Amo 1:2
b Zb 11:4; Zb 132:14
c Isa 16:9; Yer 48:33
d Isa 34:8; Ho 4:1; Ho 12:2; Mik 6:2
e Eze 18:30; Eze 20:35; Yoe 3:2
f Met 2:22; Isa 66:16; Amo 9:10
g Isa 34:2; Yer 25:17
h Isa 30:30; Isa 66:15; Yer 23:19; Yer 30:23; Sef 3:8
i Isa 34:3; Isa 66:16; Yer 12:12
j Zb 79:3; Isa 14:19
k Zb 83:10; Isa 5:25; Yer 8:2; Yer 9:22
l Yer 4:8
m Yer 6:26
n Eze 34:17
o Isa 33:1
p Yer 22:28
q Yer 32:4; Yer 52:8; Amo 2:14

Safu ya 2
a Isa 27:10
b Ho 5:14
c Yer 25:12

SURA 26
d 2Fa 23:34; 2Nya 36:4; Yer 1:3; Yer 25:1; Yer 35:1; Yer 36:1
e Yer 19:14; Yoh 18:20; Mdo 5:20
f Isa 58:1; Yer 1:7
g Kum 4:2; Mdo 20:27; Ufu 22:19
h Isa 1:16; Isa 55:7; Yer 36:3; Eze 18:27
i 1Fa 21:29; Yer 18:8
j Law 26:14; Kum 28:15
k Yer 44:10
l 2Fa 17:13; Yer 7:13; Yer 11:7; Yer 25:3
m Zb 78:60; Yer 7:12
n Yer 24:9

7 Na makuhani na manabii
na watu wote wakaanza kumsi-
kia Yeremia akisema maneno
hayo ndani ya nyumba ya Ye-
hova.[a] **8** Basi ikawa kwamba
Yeremia alipokuwa amemali-
za kusema yote ambayo Ye-
hova alimwamuru kuwaambia
watu wote, ndipo makuhani
na manabii na watu wote waka-
mkamata, wakisema: "Hakika
utakufa.[b] **9** Kwa nini ume-
toa unabii katika jina la Yeho-
va, ukisema, 'Nyumba hii ita-
kuwa kama ile iliyo katika Shi-
lo,[c] nalo jiji hili litafanywa uki-
wa hivi kwamba halitakuwa na
mkaaji'?" Na watu wote waka-
endelea kujikutanisha kumzu-
nguka Yeremia ndani ya nyu-
mba ya Yehova.

10 Baada ya muda wakuu
wa Yuda wakasikia mane-
no hayo, nao wakatoka katika
nyumba ya mfalme wakapanda
kwenda katika nyumba ya Ye-
hova[d] na kuketi katika mwi-
ngilio wa lango jipya la Yeho-
va.[e] **11** Na makuhani na ma-
nabii wakaanza kuwaambia
wakuu na watu wote: "Mtu
huyu anastahili hukumu ya
kifo,[f] kwa sababu ametoa una-
bii kulihusu jiji hili kama mli-
vyosikia kwa masikio yenu we-
nyewe."[g]

12 Ndipo Yeremia akawa-
ambia wakuu wote na watu
wote: "Yehova ndiye aliyenitu-
ma kutoa unabii kuihusu nyu-
mba hii na kulihusu jiji hili
maneno yote ambayo mmeyasi-
kia.[h] **13** Na sasa fanyeni njia
zenu na matendo yenu yawe
mema,[i] na mwitii sauti ya Ye-
hova Mungu wenu, na Yehova
ataujuta msiba ambao amese-
ma juu yenu.[j] **14** Na kwa ha-
bari yangu, tazama, mimi nipo
hapa mkononi mwenu.[a] Nite-
ndeeni kulingana na yaliyo
mema na kulingana na yaliyo
sawa machoni penu.[b] **15** Ila
tu mnapaswa kujua kabisa
kwamba, ikiwa mnaniua, ni
damu isiyo na hatia ambayo
mnajiletea juu yenu wenyewe
na juu ya jiji hili na juu ya wa-
kaaji wake,[c] kwa maana kwa
kweli Yehova alinituma kwenu
niseme masikioni mwenu ma-
neno haya yote."[d]

16 Ndipo wakuu[e] na watu
wote wakawaambia makuhani
na manabii: "Hakuna hukumu
ya kifo anayostahili mtu huyu,[f]
kwa maana alisema nasi katika
jina la Yehova Mungu wetu."[g]

17 Na zaidi ya hayo, watu
fulani kati ya wanaume wazee
wa nchi wakasimama na kua-
nza kuliambia kutaniko lote
la watu:[h] **18** "Mika[i] wa Mo-
reshethi[j] alikuwa akitoa una-
bii katika siku za Hezekia mfa-
lme wa Yuda[k] naye akawaa-
mbia watu wote wa Yuda, 'Ye-
hova wa majeshi amesema hivi:
"Sayuni utalimwa kama sha-
mba,[l] na Yerusalemu litakuwa
marundo ya mabomoko,[m] na
mlima wa ile Nyumba utaku-
wa kama mahali pa juu pa msi-
tu."'[n] **19** Je, Hezekia mfa-
lme wa Yuda na wale wote wa
Yuda walimuua? Je, hakumwo-
gopa Yehova na kuanza kuutu-
liza uso wa Yehova,[o] hivi kwa-
mba Yehova akajuta ule msi-
ba ambao alikuwa ametangaza
juu yao?[p] Basi sisi tunajifanyia
msiba mkubwa juu ya nafsi
zetu.[q]

20 "Na pia palikuwa na mtu
aliyekuwa akitoa unabii kati-
ka jina la Yehova, Uriya mwana

SURA 26
a Yer 26:2
b Zb 37:32
Amo 5:10
c Zb 78:60
d Yer 38:4
e 2Fa 15:35
2Nya 27:3
Yer 36:10
f Yer 18:20
Mt 26:66
g Yer 26:2
Yer 38:4
h Yer 1:17
i Yer 7:3
Yer 35:15
j Zb 103:10
Yer 18:8
Yer 36:3
Eze 18:32
Yon 3:9

Safu ya 2
a Yos 9:25
Yer 38:5
b 2Sa 15:26
c Hes 35:33
Kum 19:10
Met 6:17
d Yer 1:17
Yer 26:2
e Yer 36:19
f Met 16:7
Yer 38:9
g Yak 5:10
h Mdo 5:34
i Mik 1:1
j Mik 1:14
k 2Nya 29:1
l Zb 79:1
m Yer 9:11
n Mik 3:12
o 2Nya 32:26
p Kut 32:14
2Sa 24:16
q Hes 35:33
Mdo 5:39

wa Shemaya kutoka Kiriath-
yearimu.[a] Naye aliendelea ku-
toa unabii juu ya jiji hili na juu
ya nchi hii sawasawa na ma-
neno yote ya Yeremia. **21** Na
Mfalme Yehoyakimu[b] na wa-
naume wake wote wenye ngu-
vu na wakuu wote wakaya-
sikia maneno yake, na mfa-
lme akaanza kutafuta kumu-
ua.[c] Uriya aliposikia habari
hizo, akaogopa[d] mara moja,
akakimbia, akaingia Misri.
22 Lakini Mfalme Yehoyaki-
mu akatuma watu Misri, Elna-
thani mwana wa Akbori[e]
na watu wengine pamoja naye
mpaka Misri. **23** Nao waka-
mleta Uriya kutoka Misri na
kumleta kwa Mfalme Yehoya-
kimu, kisha akampiga na ku-
muua kwa upanga[f] na kuitupa
maiti yake katika makaburi ya
wana wa watu."

24 Zaidi ya hayo, mkono wa
Ahikamu[g] mwana wa Shafani[h]
ndio uliokuwa pamoja na Ye-
remia, asitiwe mkononi mwa
watu ili auawe.[i]

27 Katika mwanzo wa ufa-
lme wa Yehoyakimu
mwana wa Yosia,[j] mfalme wa
Yuda, neno hili lilimjia Yere-
mia kutoka kwa Yehova, na
kusema: **2** "Yehova ameniam-
bia hivi, 'Jitengenezee pingu
na nira,[k] nawe uziweke juu ya
shingo yako.[l] **3** Nawe uzipe-
leke kwa mfalme wa Edomu[m]
na kwa mfalme wa Moabu[n] na
kwa mfalme wa wana wa Amo-
ni[o] na kwa mfalme wa Tiro[p]
na kwa mfalme wa Sidoni[q] kwa
mkono wa wajumbe wanaokuja
Yerusalemu kwa Sedekia mfa-
lme wa Yuda. **4** Nawe uwape
amri kwa ajili ya mabwana
wao, na kusema:

SURA 26
a Yos 15:60
Yos 18:14
1Sa 7:2
b 2Fa 23:34
2Nya 36:5
c 2Nya 16:10
d 1Fa 19:3
Met 29:25
Mt 10:28
e 2Fa 22:12
Yer 36:12
f Yer 2:30
Mt 23:31
1Th 2:15
g 2Fa 22:12
2Nya 34:20
Yer 39:14
Yer 40:5
h 2Fa 22:10
i 1Fa 18:4
Mdo 23:10

SURA 27
j 2Fa 23:24
k Yer 28:10
l Eze 4:1
Eze 24:3
m Eze 25:12
Amo 1:9
Oba 1
n 2Fa 3:4
Yer 48:1
Eze 25:8
Amo 2:1
o Yer 25:21
Yer 49:1
Eze 25:2
Amo 1:13
p Isa 23:1
Yer 47:4
Eze 26:3
Amo 1:10
Zek 9:3
q Isa 23:4
Yer 25:22
Eze 28:21
Yoe 3:4

Safu ya 2
a Kut 5:1
Yer 10:10
b Zb 102:25
Zb 115:15
Zb 146:6
Isa 44:24
Isa 45:12
Yer 51:19
c Mwa 1:26
Mwa 2:7
Isa 42:5
Mdo 17:26
d Mwa 1:24
e Mwa 1:2
f Zb 136:12
Yer 32:17
g Mwa 1:29
Zb 115:16
Da 4:17
h Yer 28:14
Da 2:37
i Yer 25:9
Yer 43:10
Eze 29:18
j Zb 50:10
Yer 28:14
Da 2:38
k 2Nya 36:20
Yer 25:11

"'"Yehova wa majeshi, Mu-
ngu wa Israeli,[a] amesema
hivi; waambieni hivi mabwa-
na wenu, **5** 'Mimi mwenye-
we nimeifanya dunia,[b] wanada-
mu[c] na wanyama[d] walio juu ya
uso wa dunia kwa nguvu zangu
kuu[e] na kwa mkono wangu
ulionyooshwa;[f] nami nimempa
hiyo yeye ambaye nimemwona
kuwa sawa machoni pangu.[g]
6 Na sasa mimi mwenyewe ni-
mezitia nchi hizi zote mkono-
ni mwa Nebukadneza mfalme
wa Babiloni,[h] mtumishi wa-
ngu;[i] na nimempa hata wanya-
ma wa mwituni ili wamtumi-
kie.[j] **7** Na mataifa yote lazi-
ma wamtumikie yeye[k] na mwa-
na wake na mjukuu wake
mpaka uje wakati wa nchi yake
mwenyewe,[l] na mataifa mengi
na wafalme wakuu watamtu-
mikisha kama mtumishi.'[m]

8 """Na itatukia kwamba
lile taifa na ule ufalme ambao
hautamtumikia Nebukadne-
za mfalme wa Babiloni; na lile
ambalo halitatia shingo yake
chini ya nira ya mfalme wa Ba-
biloni, nitakaza fikira zangu
juu ya taifa hilo kwa upanga[n]
na kwa njaa[o] na kwa tauni,'[p]
asema Yehova, 'mpaka nitaka-
pokuwa nimewamaliza kabisa
kwa mkono wake.'[q]

9 """Nanyi msiwasikilize
manabii[r] wenu na waaguzi
wenu na waota-ndoto[s] wenu
na watu wenu wenye kufa-
nya uchawi na walozi[t] wenu,
ambao wanawaambia: "Ninyi
hamtamtumikia mfalme wa Ba-
biloni."[u] **10** Kwa maana wao

l Zb 137:8; Yer 25:12; Yer 50:14; Yer 50:27; Da 5:26; **m** Yer 25:14; Yer 51:11; **n** 2Fa 25:7; Yer 21:9; Yer 42:16; Eze 26:8; **o** 2Fa 25:3; Omb 4:9; **p** Yer 32:24; **q** Yer 24:10; **r** Kum 18:20; Isa 8:19; **s** Yer 29:8; **t** Isa 47:12; **u** Yer 28:2; Yer 28:11.

wanawatolea unabii wa uwongo, kusudi mpelekwe mbali kutoka katika nchi yenu; nami niwatawanye, nanyi mwangamie.[a]

11 “““Nalo taifa litakalotia shingo yake chini ya nira ya mfalme wa Babiloni na kwa kweli limtumikie, mimi pia nitaliacha lipumzike juu ya nchi yake,’ asema Yehova, ‘nalo hakika litailima na kukaa ndani yake.’”””[b]

12 Hata Sedekia[c] mfalme wa Yuda nilimwambia kulingana na maneno haya yote,[d] nikisema: “Tieni shingo zenu chini ya nira ya mfalme wa Babiloni, mkamtumikie yeye na watu wake, mwendelee kuishi.[e] **13** Kwa nini wewe mwenyewe na watu wako mfe kwa upanga,[f] kwa njaa[g] na kwa tauni[h] kulingana na yale ambayo Yehova amesema kuhusu lile taifa ambalo halitamtumikia mfalme wa Babiloni? **14** Nanyi msiyasikilize maneno ya manabii wanayowaambia, ‘Hamtamtumikia mfalme wa Babiloni,’[i] kwa sababu wanawatolea unabii wa uwongo.[j]

15 “‘Kwa maana mimi sikuwatuma,’ asema Yehova, ‘lakini wanatoa unabii katika jina langu kwa uwongo, kusudi niwatawanye,[k] nanyi mwangamie,[l] ninyi pamoja na wale manabii wanaowatolea unabii.’”[m]

16 Nami nikawaambia makuhani na watu hawa wote, nikisema: “Yehova amesema hivi, ‘Msiyasikilize maneno ya manabii wenu wanaowatolea unabii, wakisema: “Tazama! Vyombo vya nyumba ya Yehova vitarudishwa kutoka Babiloni hivi karibuni!”[a] Kwa maana wanawatolea ninyi unabii wa uwongo.[b] **17** Msiwasikilize. Mtumikieni mfalme wa Babiloni, mwendelee kuishi.[c] Kwa nini jiji hili liwe ukiwa?[d] **18** Lakini ikiwa wao ni manabii na ikiwa wana neno la Yehova, tafadhali, acheni wamwombe Yehova wa majeshi,[e] ili vyombo vilivyobaki katika nyumba ya Yehova na katika nyumba ya mfalme wa Yuda na katika Yerusalemu visiende Babiloni.’

19 “Kwa maana Yehova wa majeshi amesema hivi kuhusu zile nguzo[f] na kuhusu ile bahari[g] na kuhusu yale mabehewa[h] na kuhusu yale mabaki ya vyombo ambavyo vimebaki katika jiji hili,[i] **20** ambavyo Nebukadneza mfalme wa Babiloni hakuchukua alipompeleka uhamishoni Yekonia[j] mwana wa Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, kutoka Yerusalemu kwenda Babiloni, pamoja na watu wote wenye vyeo wa Yuda na Yerusalemu;[k] **21** kwa maana Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi kuhusu vile vyombo ambavyo vimebaki katika nyumba ya Yehova na nyumba ya mfalme wa Yuda na Yerusalemu,[l] **22** ‘“Vitapelekwa Babiloni[m] navyo vitaendelea kuwa huko mpaka siku ile nitakapovikazia fikira,”[n] asema Yehova. “Nami nitavileta na kuvirudisha mahali hapa.”’”[o]

28 Kisha ikawa kwamba mwaka huo, katika mwanzo wa ufalme wa Sedekia[p] mfalme wa Yuda, katika mwaka wa nne, mwezi wa

SURA 27

a Yer 28:16
b Yer 38:2
Yer 40:9
Yer 42:10
c 2Fa 24:17
1Nya 3:15
2Nya 36:10
Yer 37:1
d 2Nya 36:12
e Met 1:33
Yer 38:20
f Kum 28:63
Eze 18:31
Eze 33:11
g Kum 28:53
Eze 14:21
h Kum 28:61
Yer 38:2
i Yer 37:19
j Yer 14:14
Yer 23:21
Yer 28:15
Yer 29:8
Eze 13:6
k Kum 28:64
l Law 26:38
Kum 30:18
m 1Fa 22:23
Yer 20:6
Yer 29:21
Eze 13:3

Safu ya 2

a 2Fa 24:13
2Nya 36:7
Yer 28:3
Da 1:2
b Yer 14:13
c Yer 27:11
d Law 26:33
Yer 38:17
Yer 38:23
e 1Fa 18:24
Yer 7:16
f 1Fa 7:15
2Fa 25:17
2Nya 4:12
Yer 52:21
g 1Fa 7:23
2Fa 25:13
h 1Fa 7:27
2Fa 25:16
2Nya 4:14
Yer 52:17
i 2Fa 25:14
2Nya 36:18
j 2Fa 24:15
2Nya 36:10
Yer 22:28
k 2Fa 24:14
Yer 24:1
Yer 29:1
Da 1:3
l 2Nya 36:10
m 2Fa 25:13
2Nya 36:18
Yer 52:18
Da 5:3
n 2Nya 36:21
Ezr 1:7
Yer 29:10
o Kum 30:3
Ezr 5:14
Ezr 7:19

SURA 28

p 2Fa 24:17
2Nya 36:10

tano, Hanania[a] mwana wa Azuri, yule nabii kutoka Gibeoni,[b]
akaniambia hivi ndani ya nyumba ya Yehova mbele ya macho
ya makuhani na ya watu wote:
2 "Yehova wa majeshi, Mungu
wa Israeli, amesema hivi, 'Nitaivunja nira ya mfalme wa Babiloni.[c] **3** Katika muda wa miaka miwili kamili nitavirudisha
mahali hapa vyombo vyote vya
nyumba ya Yehova ambavyo
Nebukadneza mfalme wa Babiloni[d] alivichukua kutoka mahali hapa ili kuvipeleka Babiloni.'" **4** "'Na Yekonia[e] mwana wa Yehoyakimu,[f] mfalme
wa Yuda, pamoja na wahamishwa wote wa Yuda ambao wameenda Babiloni[g] nitawarudisha tena mahali hapa,' asema
Yehova, 'kwa maana nitaivunja
nira[h] ya mfalme wa Babiloni.'"

5 Na Yeremia nabii akamwambia Hanania nabii mbele ya
macho ya makuhani na mbele
ya macho ya watu wote waliokuwa wamesimama ndani ya
nyumba ya Yehova;[i] **6** ndiyo,
Yeremia nabii akasema: "Amina![j] Yehova na afanye hivyo!
Yehova na ayatimize maneno yako ambayo umetoa unabii kwa kuvirudisha tena mahali hapa kutoka Babiloni vyombo vya nyumba ya Yehova
na watu wote waliohamishwa![k]
7 Hata hivyo, tafadhali sikia
neno hili ninalosema masikioni mwako na masikioni mwa
watu wote.[l] **8** Kwa habari ya
manabii walionitangulia mimi
na waliokutangulia wewe kutoka zamani za kale,[m] wao pia
walikuwa wakitoa unabii kuhusu nchi nyingi na kuhusu
falme kubwa, juu ya vita na
juu ya msiba na juu ya tauni.[n]

SURA 28

a Yer 28:11
b Yos 11:19
2Sa 21:2
c Yer 27:8
Mik 3:11
d 2Fa 24:13
Yer 27:16
Da 1:2
e 2Fa 24:8
2Fa 25:27
Est 2:6
Yer 22:24
Yer 37:1
f 2Fa 23:36
2Fa 24:6
g 2Fa 24:14
Yer 24:1
h Yer 30:8
i Yer 7:2
Yer 19:14
Yer 26:2
j 1Fa 1:36
Zb 41:13
Yer 11:5
2Ko 1:20
k Yer 28:3
l 1Fa 22:28
m Kum 4:26
Kum 28:15
n 1Fa 22:8
Yon 3:6

Safu ya 2

a Yer 6:14
Yer 14:13
Eze 13:10
b Kum 18:22
c Zb 10:13
Yer 27:2
d Yer 28:1
e 1Fa 13:18
2Nya 18:10
Yer 23:17
Yer 29:9
f Yer 28:4
g Met 14:7
Met 26:4
h Yer 29:30
i Yer 27:2
Yer 28:10
j Kum 28:48
k Kum 28:49
l Kum 28:48
Yer 5:19
Yer 27:7
m Yer 27:6
Da 2:38
n Yer 28:1
o Kum 13:1
Yer 14:14
Yer 23:21
Yer 27:15
Yer 29:31
Eze 13:3
Zek 13:3
Lu 6:26

9 Kwa habari ya nabii anayetoa unabii wa amani,[a] wakati neno la nabii huyo litakapotimia yule nabii ambaye Yehova amemtuma kikweli atajulikana."[b]

10 Ndipo Hanania nabii akaichukua ile nira kutoka shingoni mwa Yeremia nabii na
kuivunja.[c] **11** Na Hanania[d]
akasema mbele ya macho ya
watu wote: "Yehova amesema hivi,[e] 'Hivi ndivyo nitakavyoivunja nira ya Nebukadneza mfalme wa Babiloni katika
muda wa miaka miwili kamili
ili itoke shingoni mwa mataifa
yote.'"[f] Na Yeremia nabii akaenda zake.[g]

12 Ndipo neno la Yehova
likamjia Yeremia,[h] baada ya Hanania nabii kuivunja ile nira
kutoka shingoni mwa Yeremia
nabii, na kusema: **13** "Nenda, umwambie Hanania, 'Yehova amesema hivi: "Umevunja nira[i] za miti, na badala ya
hizo utatengeneza nira za chuma."[j] **14** Kwa maana Yehova
wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi: "Nitatia nira
ya chuma juu ya shingo ya mataifa haya yote, ili yamtumikie
Nebukadneza mfalme wa Babiloni;[k] nao lazima watamtumikia.[l] Nami nitampa hata wanyama wa mwituni."'"[m]

15 Na Yeremia nabii akaendelea kumwambia Hanania[n]
nabii: "Tafadhali, sikiliza, Ee Hanania! Yehova hakukutuma wewe, bali wewe
mwenyewe umewafanya watu
hawa wautegemee uwongo.[o]
16 Kwa hiyo Yehova amesema hivi, 'Tazama! Ninakuondolea mbali kutoka katika uso
wa nchi. Mwaka huu utakufa

hakika,[a] kwa maana umesema maasi ya waziwazi juu ya Yehova.'"[b]

17 Basi Hanania nabii akafa mwaka huo, katika mwezi wa saba.[c]

29 Na haya ndiyo maneno ya barua ambayo Yeremia nabii alituma kutoka Yerusalemu kwa mabaki ya wanaume wazee wa watu waliohamishwa na kwa makuhani na kwa manabii na kwa watu wote, ambao Nebukadneza alikuwa amewapeleka uhamishoni kutoka Yerusalemu kwenda Babiloni[d] **2** baada ya Yekonia[e] mfalme na malkia[f] na maofisa wa makao ya mfalme, wakuu wa Yuda na Yerusalemu,[g] na mafundi na wajenzi wa maboma[h] kwenda kutoka katika Yerusalemu. **3** Ilikuwa kwa mkono wa Elasa mwana wa Shafani[i] na Gemaria mwana wa Hilkia, ambao Sedekia[j] mfalme wa Yuda aliwatuma kwenda Babiloni kwa Nebukadneza mfalme wa Babiloni, na kusema:

4 "Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amewaambia hivi watu wote waliohamishwa, ambao nimewapeleka uhamishoni[k] kutoka Yerusalemu kwenda Babiloni, **5** 'Jengeni nyumba na kukaa ndani yake, mpande bustani na kula matunda yake.[l] **6** Chukueni wake na kuzaa wana na binti;[m] na kuwachukulia wana wenu wake na kuwaoza binti zenu kwa waume, ili wazae wana na binti; na muwe wengi huko, wala msiwe wachache. **7** Pia, tafuteni amani kwa ajili ya jiji ambamo nimewapeleka ninyi uhamishoni, nanyi msali kwa ajili yake kwa Yehova, kwa maana katika amani ya jiji hilo kutakuwa na amani kwa ajili yenu wenyewe.[a] **8** Kwa maana Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi: "Msiache manabii wenu walio katikati yenu na waaguzi wenu wawadanganye,[b] nanyi msisikilize ndoto zao ambazo wanaota.[c] **9** Kwa maana 'wanawatolea ninyi unabii wa uwongo katika jina langu. Mimi sikuwatuma,'[d] asema Yehova."""

10 "Kwa maana Yehova amesema hivi, 'Kupatana na kutimia kwa miaka 70 katika Babiloni nitawakazia ninyi fikira,[e] nami nitawatimizia neno langu jema kwa kuwarudisha tena mahali hapa.'[f]

11 "'Kwa maana mimi najua vema mawazo ninayofikiria kuwaelekea ninyi,'[g] asema Yehova, 'mawazo ya amani, wala si ya msiba,[h] ili kuwapa ninyi wakati ujao na tumaini.[i] **12** Na hakika mtaniita na kuja na kusali kwangu, nami nitawasikiliza.'[j]

13 "'Nanyi kwa kweli mtanitafuta na kunipata,[k] kwa maana mtanitafuta kwa moyo wenu wote.[l] **14** Nami nitajiacha mnipate,'[m] asema Yehova. 'Nami nitakusanya kundi lenu la mateka na kuwakusanya ninyi pamoja kutoka katika mataifa yote na kutoka katika mahali pote ambapo nimewatawanya ninyi,'[n] asema Yehova. 'Nami nitawarudisha katika mahali ambapo kutoka hapo niliwapeleka uhamishoni.'[o]

15 "Lakini mmesema, 'Yehova ametuinulia manabii katika Babiloni.'

SURA 28

a Kum 18:20
1Sa 2:34
b Kum 13:5
Yer 29:32
c 2Fa 7:17

SURA 29

d 2Fa 24:15
Yer 24:1
e 2Fa 24:8
2Nya 36:9
Yer 22:24
Yer 27:20
Yer 28:4
f 2Fa 24:12
Yer 22:26
g 2Fa 24:14
h 2Fa 24:16
i 2Fa 22:8
Yer 26:24
Yer 39:14
Eze 8:11
j 2Fa 24:18
2Nya 36:11
k Kum 28:41
Yer 24:5
l Yer 29:28
m Mwa 1:28
Mwa 9:7

Safu ya 2

a Ezr 6:10
Ezr 7:23
1Ti 2:2
b Yer 14:14
Yer 23:21
Yer 27:14
Efe 5:6
c Kum 13:3
d Yer 23:21
Yer 28:15
e 2Nya 36:21
Ezr 1:1
Yer 27:22
Da 9:2
Zek 1:12
Zek 7:5
f Kum 30:3
Ezr 2:1
Yer 24:6
g Ayu 23:13
Zb 33:11
Zb 40:5
h Sef 3:15
i Yer 31:17
j Zb 10:17
Isa 30:19
Da 9:3
Yoh 9:31
k Law 26:40
1Fa 8:47
Mt 7:7
l Kum 4:29
Kum 30:2
1Fa 8:48
Yer 24:7
m Kum 4:7
Isa 55:6
n Kum 30:4
Isa 49:25
Yer 23:3
Yer 30:3
Eze 39:28
Yoe 3:1
o Zb 126:1
Ho 6:11
Amo 9:14
Sef 3:20

16 "Kwa maana Yehova
amesema hivi kwa mfalme anayeketi juu ya kiti cha ufalme
cha Daudi[a] na kwa watu wote
wanaokaa katika jiji hili, ndugu zenu ambao hawakwenda
pamoja nanyi uhamishoni,[b]
17 'Yehova wa majeshi amesema hivi: "Tazama, ninatuma
juu yao upanga,[c] njaa[d] na tauni,[e] nami nitawafanya kuwa
kama tini zilizopasuka ambazo haziwezi kuliwa kwa sababu ya
ubaya."'[f]
18 "'Nami nitawafuatilia
kwa upanga, kwa njaa na kwa
tauni, nami nitawatoa wawe
kitu cha kutetemesha falme
zote za dunia,[g] kuwa laana na
kuwa kitu cha kushangaza na
kuwa kitu cha kupigiwa mluzi na kuwa kitu cha kushutumiwa katikati ya mataifa yote
ambako hakika nitawatawanya,[h] **19** kwa sababu hawa-
kuyasikiliza maneno yangu,'
asema Yehova, 'ambayo nimetuma kwao kupitia watumishi
wangu manabii, nikiamka mapema na kuwatuma.'[i]
"'Lakini hamkusikiliza,'[j] asema Yehova.
20 "Nanyi sikieni neno la Yehova, ninyi nyote mliohamishwa,[k] ambao nimewafukuza kutoka Yerusalemu kwenda
Babiloni.[l] **21** Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema
hivi kumhusu Ahabu mwana
wa Kolaya na kumhusu Sedekia mwana wa Maaseya, ambao
wanawatolea ninyi unabii wa
uwongo katika jina langu mwenyewe,[m] 'Tazama, nitawatia
mkononi mwa Nebukadreza
mfalme wa Babiloni, naye
atawapiga na kuwaua mbele
ya macho yenu.[n] **22** Na kuto-
ka kwao hakika laana itachukuliwa na kundi zima la waha-
mishwa walio katika Babiloni,
na kusema: "Yehova na akufanye kama Sedekia na kama
Ahabu,[a] ambao mfalme wa
Babiloni aliwachoma motoni!"[b] **23** kwa sababu wamete-
nda upumbavu katika Israeli,[c] nao wanaendelea kufanya
uzinzi pamoja na wake za wenzao[d] na kuendelea kusema
uwongo kwa jina langu mwenyewe neno ambalo mimi sikuwaamuru.[e]
"'"Mimi ndiye ninayejua
nami ni shahidi,"[f] asema Yehova.'"
24 "Nawe utamwambia hivi
Shemaya[g] wa Nehelamu,
25 'Yehova wa majeshi, Mungu
wa Israeli, amesema hivi: "Kwa
sababu wewe umetuma barua[h] katika jina lako kwa watu
wote walioko Yerusalemu, na
kwa Sefania[i] mwana wa Maaseya, kuhani, na kwa maku-
hani wote, ukisema, **26** 'Yehova amekufanya wewe kuwa
kuhani badala ya Yehoyada
kuhani, ili uwe mwangalizi
mkuu wa nyumba ya Yehova[j]
kuelekea mtu yeyote aliyetiwa wazimu[k] na mwenye kujie-
ndesha kama nabii, nawe uta-
mtia katika mikatale na katika kongwa;[l] **27** sasa, basi,
kwa nini hukumkemea Yeremia wa Anathothi,[m] ambaye
anajiendesha kama nabii kwenu?[n] **28** Kwa maana ndiyo sa-
babu ametuma ujumbe kwetu Babiloni, akisema: "Ni wa
muda mrefu! Jengeni nyumba
na kukaa ndani yake, na kupanda bustani na kula matunda yake,[o] — """"

SURA 29

a Yer 22:2
Yer 28:1
b 2Fa 24:14
c Law 26:33
Yer 24:10
d Kum 28:53
Yer 15:2
e Kum 28:61
Yer 34:17
f Yer 24:2
Yer 24:8
g Law 26:33
Kum 28:25
2Nya 29:8
Yer 15:4
Yer 24:10
Yer 34:17
h Kum 29:24
1Fa 9:8
2Nya 7:21
Zb 44:11
Yer 24:9
Yer 25:9
Omb 2:15
i Yer 7:13
Yer 25:4
Yer 32:33
j Yer 6:19
Yer 26:5
Mdo 28:27
k 2Fa 24:14
l Yer 24:5
Mik 4:10
m Yer 14:14
Yer 29:8
Omb 2:14
2Pe 2:1
n Yer 52:27

Safu ya 2

a Kum 29:20
Isa 65:15
b Da 3:6
c Yer 23:14
d Yer 7:9
Ho 4:2
e Yer 27:15
f Met 5:21
Yer 16:17
Yer 23:24
Mal 3:5
Ebr 4:13
g Yer 29:31
h 1Fa 21:8
2Nya 32:17
Ne 6:5
i 2Fa 25:18
Yer 21:1
Yer 29:29
Yer 37:3
Yer 52:24
j Hes 3:32
Hes 4:16
Yer 20:1
k 2Fa 9:11
Ho 9:7
l 2Nya 16:10
Yer 20:2
Mdo 16:24
m Yer 1:1
n 1Sa 10:6
1Sa 19:20
Yer 43:2
o Yer 29:5

29 Na Sefania[a] kuhani akaisoma barua hii masikioni mwa
Yeremia nabii.
30 Ndipo neno la Yehova likamjia Yeremia, na kusema:
31 "Tuma ujumbe kwa watu
wote waliohamishwa,[b] ukisema, 'Yehova amesema hivi kumhusu Shemaya wa Nehelamu:
"Kwa sababu Shemaya amewatolea ninyi unabii, lakini mimi
mwenyewe sikumtuma, naye alijaribu kuwafanya mtegemee uwongo,[c] **32** basi Yehova amesema hivi, 'Tazama, ninakaza fikira zangu juu ya Shemaya[d] wa Nehelamu na juu ya
uzao wake.'[e]
"""'Hatakuwa na mtu anayekaa katikati ya kikundi
hiki cha watu;[f] wala hatautazama wema ambao nitawafanyia
watu wangu,'[g] asema Yehova, 'kwa maana amesema maasi ya
waziwazi juu ya Yehova.'"""[h]

30 Neno lililomjia Yeremia
kutoka kwa Yehova, na
kusema: **2** "Yehova Mungu
wa Israeli amesema hivi, 'Andika katika kitabu maneno yote
nitakayokuambia.[i] **3** Kwa
maana, "tazama! siku zinakuja," asema Yehova, "nami nitawakusanya mateka wa watu
wangu, Israeli na Yuda,"[j] Yehova amesema, "nami nitawarudisha katika nchi niliyowapa
mababu zao, nao hakika wataimiliki tena."'"[k]
4 Na haya ndiyo maneno
ambayo Yehova amewaambia
Israeli na Yuda. **5** Kwa maana Yehova amesema hivi: "Sauti ya kutetemeka tumeisikia, hofu,[l] na hakuna amani.
6 Ulizeni, tafadhali, na mwone ikiwa mwanamume anajifungua mtoto. Kwa nini nimemwona kila mwanamume
akiweka mikono juu ya viuno
vyake kama mwanamke anayejifungua mtoto,[a] na nyuso zote
zimegeuka rangi?[b] **7** Ole wangu! Kwa maana siku ile ni
kuu,[c] hivi kwamba hakuna nyingine kama hiyo,[d] na ni wakati wa taabu kwa Yakobo.[e]
Lakini yeye ataokolewa kutoka katika hiyo."
8 "Na itakuwa katika siku
hiyo," asema Yehova wa majeshi, "kwamba nitaivunja nira
ya mtu kutoka shingoni mwako, na pingu zako nitazikata vipande viwili,[f] na wageni
hawatamtumia vibaya tena
kama mtumishi. **9** Nao hakika watamtumikia Yehova Mungu wao na Daudi mfalme
wao,[g] ambaye nitawasimamishia."[h]
10 "Nawe usiogope, Ee mtumishi wangu Yakobo," asema
Yehova, "wala usiingiwe na
hofu, Ee Israeli.[i] Kwa maana, tazama, ninakuokoa wewe
kutoka mbali na uzao wako kutoka katika nchi yao ya utekwani.[j] Na hakika Yakobo atarudi na kuwa huru kutokana
na usumbufu naye atastarehe,
wala hakutakuwa na mtu yeyote anayemtetemesha."[k]
11 "Kwa maana mimi niko
pamoja nawe," asema Yehova, "ili nikuokoe;[l] lakini nitafanya maangamizi kati ya mataifa yote ambako nimekutawanya.[m] Hata hivyo, kwako
sitafanya maangamizi.[n] Nami
nitakurekebisha kwa kiwango
kinachofaa, kwa kuwa sitakuacha kamwe bila kukuadhibu."[o]

SURA 29
a 2Fa 25:18; Yer 21:1; Yer 52:24
b 2Fa 24:14; Yer 29:20
c Yer 14:14; Yer 23:21; Yer 28:15; Eze 13:8; 2Pe 2:1
d Yer 29:24
e Kut 20:5; Kut 34:7; Yer 20:6
f 1Sa 2:30
g Met 12:19
h Yer 28:16

SURA 30
i Yer 36:2; Yer 51:60; Da 7:1; Hab 2:2; Ro 15:4
j Kum 30:3; Zb 53:6; Yer 27:22; Yer 29:14; Eze 39:25; Yoe 3:1; Amo 9:14
k Yos 14:1; Ezr 2:1; Yer 16:15; Yer 32:44; Eze 20:42
l Yer 6:23

Safu ya 2
a Isa 13:8; Yer 4:31; Yer 6:24; Mik 4:9
b Isa 29:22
c Yoe 2:11; Amo 5:18; Sef 1:14
d Omb 1:12; Da 12:1; Mt 24:21
e Ho 12:2
f Isa 9:4; Isa 10:27
g Isa 55:3; Eze 34:23; Ho 3:5
h Eze 37:24; Lu 1:69; Mdo 2:30; Mdo 13:23
i Isa 41:13; Isa 43:5; Isa 44:2
j Isa 49:25; Yer 3:18
k Yer 33:16; Yer 46:27; Eze 34:25; Ho 2:18; Mik 4:4
l Yer 46:27; Eze 11:17
m Isa 47:11; Yer 50:29; Yer 51:24
n Law 26:44; Ne 9:31; Zb 78:38; Omb 3:22; Eze 20:17; Amo 9:8
o Kut 34:7; Zb 6:1; Yer 10:24; Yer 46:28

12 Kwa maana Yehova amesema hivi: "Hakuna matibabu
kwa ajili ya kuvunjika kwako.[a] Pigo lako ni la kudumu.[b]
13 Hakuna yeyote anayetetea mambo yako, kidonda cha-
ko.[c] Hakuna njia ya kuponya,
hakuna matibabu, kwa ajili
yako.[d] **14** Wale wote wanao-
kupenda sana ndio wale ambao
wamekusahau.[e] Si wewe amba-
ye wanaendelea kukutafuta.
Kwa maana nimekupiga kwa
pigo la adui,[f] kwa adhabu
ya mtu mkatili,[g] kwa sababu ya
wingi wa makosa yako;[h] dha-
mbi zako zimekuwa nyingi.[i]
15 Kwa nini unapaaza kilio
kwa sababu ya kuvunjika kwa-
ko?[j] Maumivu yako hayawezi
kupona kwa sababu ya wingi
wa makosa yako;[k] dhambi zako
zimekuwa nyingi. Nimekute-
ndea mambo hayo. **16** Kwa
hiyo wale wote wanaokumeza
nao wenyewe watamezwa;[l] nao
adui zako wote, wote wataenda utekwani.[m] Na wale wana-
okupora hakika wataporwa, na
wale wote wanaokunyakua ni-
tawatoa wanyakuliwe."[n]
17 "Kwa maana nitakurudi-
shia afya, nami nitakuponya
mapigo yako,"[o] asema Yehova.
"Kwa maana walikuita mwa-
namke aliyefukuzwa:[p] 'Huyo
ni Sayuni, ambaye hakuna ye-
yote anayemtafuta.'"[q]
18 Yehova amesema hivi:
"Tazama, ninawakusanya ma-
teka wa mahema ya Yakobo,[r]
nami nitazihurumia maskani
zake. Na kwa kweli jiji litaje-
ngwa upya juu ya kilima cha-
ke;[s] na mnara wa makao uta-
keti juu ya mahali pake pana-
poufaa.[t] **19** Na kutoka kwao
hakika shukrani zitatolewa,
na sauti ya wale wanaocheka.[a]
Nami nitawazidisha, nao ha-
watakuwa wachache;[b] nami ni-
tawafanya kuwa wengi katika
hesabu, nao hawatakuwa wa-
nyonge.[c] **20** Na wanawe wa-
takuwa kama katika nyakati
za zamani, na kusanyiko lake
litafanywa imara mbele za-
ngu.[d] Nami nitakaza fikira za-
ngu juu ya wakandamizaji
wake wote.[e] **21** Na mtu wake
aliye mashuhuri atakuwa ku-
toka kwake,[f] na mtawala wake
atatoka katikati yake;[g] nami
nitamleta karibu, naye atani-
karibia."[h]
"Kwa maana, sasa, ni nani
huyu ambaye ametoa moyo
wake rehani ili kunikaribia?"[i]
asema Yehova. **22** "Nanyi ha-
kika mtakuwa watu wangu,[j]
na mimi nitakuwa Mungu
wenu."[k]
23 Tazama! Dhoruba ya Ye-
hova, ghadhabu, imetoka, tu-
fani inayofagia ikisonga mbe-
le.[l] Itazunguka juu ya kichwa
cha waovu.[m] **24** Hasira ya Ye-
hova inayowaka haitarudi nyu-
ma mpaka atakapokuwa ame-
fanya na mpaka atakapoku-
wa ametimiza mawazo ya moyo
wake.[n] Mtalifikiria jambo hilo
katika siku za mwisho.[o]

31 "Wakati huo," asema Ye-
hova, "Nitakuwa Mungu
kwa familia zote za Israeli; nao
watakuwa watu wangu."[p]
2 Yehova amesema hivi:
"Watu waliookoka upanga wa-
lipata kibali nyikani,[q] wakati
Israeli alipokuwa akitembea ili
kupata starehe yake."[r] **3** Ku-
toka mbali Yehova alinitokea,

SURA 30
a 2Nya 36:16 Isa 6:10 Yer 8:21
b Yer 15:18
c Zb 106:23
d Yer 8:22
e Omb 1:2 Omb 1:19
f Omb 2:5
g Kum 28:50
h Zb 38:8
i Yer 5:6
j Yer 15:18
k 2Nya 36:14 Ne 9:26
l Kut 23:22 Isa 33:1 Isa 41:11 Yer 10:25 Yer 25:12 Yer 50:29
m Yer 51:56 Mik 5:9
n Zek 2:9
o Zb 102:13 Zb 103:3 Yer 33:6 Ho 6:1
p Zb 44:13
q Ne 4:3 Omb 2:15
r Zb 85:1 Yer 24:6 Yer 29:10
s Mik 4:8
t Zb 48:3

Safu ya 2
a Ezr 3:12 Ne 8:17 Isa 35:10 Isa 51:11 Yer 31:4
b Kum 30:5 Isa 27:6 Yer 33:22 Zek 10:8
c Isa 60:22 Mik 4:7 Sef 3:19
d Zb 102:28 Isa 1:26
e Isa 49:26 Yer 50:18
f Mwa 49:10
g Isa 9:6
h Hes 16:5 Zb 110:1 Da 7:13 Mt 3:17 Ebr 9:24
i Kum 30:6 Yer 24:7 Mk 12:30 Ro 2:29 2Ti 2:22
j Eze 11:20 Ho 2:23 Ufu 21:3
k Yer 31:1 Eze 36:28 Ebr 8:10
l Met 1:27 Yer 25:32
m Amu 9:57 Met 16:4
n Ayu 23:13 Isa 14:24 Yer 4:28
o Mwa 49:1 Yer 23:20 Eze 38:8

SURA 31 p Law 26:12; Yer 30:22; Yer 31:33; Ebr 8:10; q Kum 1:31; r Hes 10:33; Zb 95:11; Isa 63:14; Ebr 4:8.

akisema: "Nimekupenda wewe
kwa upendo mpaka wakati usio
na kipimo.[a] Ndiyo sababu
nimekuvuta kwa fadhili zenye
upendo.[b] **4** Bado nitakujenga
upya nawe kwa kweli utaje-
ngwa upya,[c] Ee bikira wa Israe-
li. Bado utajipamba kwa mata-
ri yako na kwa kweli utaenda
katika dansi ya wale wanaoche-
ka.[d] **5** Bado utapanda masha-
mba ya mizabibu katika milima
ya Samaria.[e] Hakika wapandaji
watapanda na kuanza kula ma-
tunda.[f] **6** Kwa maana kuna
siku ambayo walinzi walio kati-
ka eneo lenye milima la Efraim-
u wataita, 'Simameni, twe-
nde Sayuni, kwa Yehova Mungu
wetu.'"[g]

7 Kwa maana Yehova ame-
sema hivi: "Mlilieni Yakobo
kwa sauti kubwa kwa kusha-
ngilia, na kupaaza kelele mbele
ya mataifa.[h] Tangazeni jambo
hilo.[i] Sifuni na kusema, 'Wa-
okoe, Ee Yehova, watu wako,
mabaki ya Israeli.'[j] **8** Taza-
ma, ninawaleta kutoka kati-
ka nchi ya kaskazini,[k] nami ni-
tawakusanya kutoka sehemu
za mbali zaidi za dunia.[l] Kati
yao patakuwa na vipofu na vi-
lema, mwanamke mwenye mi-
mba na yule anayezaa, wote
pamoja.[m] Watarudi hapa waki-
wa kutaniko kubwa.[n] **9** Wa-
takuja wakilia,[o] nami nitawa-
leta wakiwa na maombi yao
ya kusihi wakitaka kibali.
Nitawatembeza kwenye ma-
bonde ya mito ya maji,[p] kati-
ka njia iliyo sawa ambayo nda-
ni yake hawatakwazwa. Kwa
maana mimi nimekuwa Baba
kwa Israeli;[q] naye Efraimu,
yeye ni mzaliwa wangu wa
kwanza."[r]

SURA 31

a Kum 7:8
Mal 1:2
b Ho 11:4
c Yer 1:10
Yer 30:18
Yer 33:7
Amo 9:11
d Kut 15:20
Amu 11:34
Zb 149:3
Yer 30:19
e Amo 9:14
Mik 4:4
f Kum 30:9
Isa 65:21
g Ezr 1:5
Zb 126:1
Isa 2:3
Yer 50:5
Mik 4:2
h Kum 32:43
Zb 96:3
Isa 44:23
Ro 15:10
i Isa 12:5
Amo 3:9
Mdo 26:23
j Isa 1:9
Yer 23:3
Yoe 2:32
Ro 9:27
Ro 11:5
k Isa 43:6
Yer 3:12
Yer 23:8
l Kum 30:4
Eze 20:34
Eze 34:12
Yak 1:1
m Isa 35:6
Isa 42:16
n Ezr 2:64
o Yer 50:4
p Isa 35:7
Isa 49:10
q Kum 32:6
r Mwa 48:14
Kut 4:22

Safu ya 2

a Zb 97:1
Isa 11:11
Isa 42:10
b Kum 30:4
Eze 20:34
Mik 2:12
c Isa 40:11
Eze 34:12
1Pe 2:25
d Isa 44:23
Isa 48:20
e Isa 49:25
f Ezr 3:13
Zb 126:1
Isa 51:11
Eze 20:40
g Zb 34:5
Isa 60:5
h Yoe 3:18
Zek 9:15
i Isa 65:10
j Isa 58:11
k Isa 35:10
Ufu 21:4
l Ezr 3:12
Zek 8:4
m Isa 51:3
Isa 65:19
n Zb 36:8
o Kum 30:9
Zb 31:19
Isa 63:7
p Yos 18:25
Yer 40:1
Mt 2:18

10 Sikieni neno la Yehova,
enyi mataifa, na kulitangaza
kati ya visiwa vilivyo mbali,[a]
na kusema: "Yeye anayemta-
wanya Israeli atamkusanya pa-
moja,[b] na hakika yeye atamwe-
ka kama mchungaji anavyoli-
weka kundi lake.[c] **11** Kwa
maana kwa kweli Yehova ata-
mkomboa Yakobo[d] na kumpo-
nya kutoka mkononi mwa yule
aliye na nguvu kuliko yeye.[e]
12 Nao hakika watakuja na
kupiga vigelegele vya shangwe
juu ya kilele cha Sayuni[f] na
kung'aa kwa sababu ya wema
wa Yehova,[g] kwa sababu ya
nafaka na kwa sababu ya di-
vai[h] mpya na kwa sababu ya
mafuta na kwa sababu ya wa-
toto wa kundi na ng'ombe.[i] Na
nafsi yao itakuwa tu kama bu-
stani iliyonyweshwa maji vi-
zuri,[j] nao hawatakuwa dhaifu
tena."[k]

13 "Wakati huo bikira ata-
shangilia kwa dansi, pia vijana
na wanaume wazee, wote pa-
moja.[l] Nami nitayageuza mao-
mbolezo yao yawe furaha, nami
nitawafariji na kuwafanya wa-
shangilie kutoka katika hu-
zuni yao.[m] **14** Nami nitaishi-
bisha nafsi ya makuhani kwa
mafuta,[n] na watu wangu wata-
shiba wema,"[o] asema Yehova.

15 "Yehova amesema hivi,
'Katika Rama[p] sauti inasikiwa,
maombolezo na kilio cha uchu-
ngu;[q] Raheli[r] akiwalilia wana-
we.[s] Amekataa kufarijiwa juu
ya wanawe,[t] kwa sababu hawa-
ko tena.'"[u]

16 Yehova amesema hivi:
"'Zuia sauti yako, usilie, na
macho yako yasitoe machozi,[v]

q Omb 1:16; Mt 2:16; r Mwa 35:19; s Mwa 35:24;
t Mwa 37:35; u Mt 2:18; v Ufu 7:17.

kwa maana kuna thawabu kwa
ajili ya utendaji wako,' asema
Yehova, 'nao hakika watarudi
kutoka katika nchi ya adui.'[a]

17 "'Na kuna tumaini[b] kwa
ajili ya wakati wako ujao,' ase-
ma Yehova, 'na wana watarudi
hakika katika eneo lao wenye-
we.'"[c]

18 "Hakika nimemsikia Efra-
imu akijiombolezea,[d] 'Umeni-
rekebisha,[e] ili nipate kurekebishwa, kama ndama ambaye hajazoezwa.[f] Unigeuze mimi, nami nitageuka bila kusita,[g] kwa maana wewe ni Yehova Mungu wangu.[h] **19** Kwa maana baada ya kugeuka kwangu nilihisi kujuta;[i] na baada ya kujulishwa nililipiga paja kofi.[j] Niliona aibu, na pia nikafedheheka,[k] kwa maana nilikuwa nimechukua shutuma ya ujana wangu.'"[l]

20 "Je, Efraimu ni mwana mwenye thamani kwangu, au mtoto anayetendewa kwa upendo?[m] Kwa maana kwa kiasi ninachosema vibaya juu yake bila shaka nitamkumbuka zaidi.[n] Ndiyo sababu matumbo yangu yamekuwa na msukosuko kwa ajili yake.[o] Kwa kuwa nitamhurumia kabisa,"[p] asema Yehova.

21 "Jisimamishie alama za barabara. Jiwekee vibao vya ishara.[q] Kaza moyo wako juu ya njia kuu, njia ambayo utaiendea.[r] Rudi, Ee bikira wa Israeli. Rudi kwenye haya majiji yako.[s] **22** Utaendelea kugeuka huku na huku mpaka wakati gani,[t] Ee binti usiye mwaminifu?[u] Kwa maana Yehova ameumba jambo jipya duniani: Mwanamke atajibana kwa mwanamume."

SURA 31

a Ezr 1:5
Yer 23:3
Eze 11:17
Ho 1:11
b Yer 29:11
c Yer 46:27
d Yer 31:9
e Zb 94:12
f Met 26:3
g Yer 17:14
Omb 5:21
h Isa 43:3
i Kum 30:2
j Eze 21:12
k Law 26:41
Ezr 9:6
l Yer 3:25
m Yer 31:9
Ho 14:4
n Kum 32:36
o Isa 63:15
Ho 11:8
p Isa 55:7
Mik 7:18
2Ko 1:3
q Isa 62:10
r Isa 35:8
s Yer 3:14
t 1Fa 18:21
Yer 2:18
u Yer 2:13
Yer 3:6

Safu ya 2

a Zb 122:8
b Isa 1:26
c Zek 8:3
d Yer 33:12
Eze 36:10
e Zb 107:9
Isa 40:29
f Kum 30:9
Eze 36:9
Ho 2:23
Zek 10:9
g Yer 44:27
Da 9:14
h Yer 18:7
Yer 45:4
i Zb 102:16
Zb 147:2
Yer 24:6
Yer 32:41
j Eze 18:2
k Kum 24:16
Isa 3:11
Eze 18:4
Ga 6:7
l Mt 26:28
Mk 14:24
Lu 22:20
1Ko 11:25
Ebr 8:8
Ebr 10:16

23 Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi: "Bado watasema neno hili katika nchi ya Yuda na katika majiji yake, nitakapowakusanya mateka wao, 'Yehova na akubariki,[a] Ee makao ya uadilifu,[b] Ee mlima mtakatifu.'[c] **24** Na Yuda na majiji yake yote hakika watakaa ndani yake pamoja, wakulima na wale ambao wameondoka wakiwa na kundi.[d] **25** Kwa maana nitaishibisha nafsi iliyochoka, nami nitaijaza kila nafsi ambayo ni dhaifu."[e]

26 Ndipo nikaamka na kuanza kuona; nao usingizi wangu ulikuwa umekuwa mtamu kwangu.

27 "Tazama! Siku zinakuja," asema Yehova, "nami nitaipanda nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda uzao wa mwanadamu na uzao wa mnyama wa kufugwa."[f]

28 "Na itakuwa kwamba kama nilivyokuwa macho kuwaelekea wao[g] ili kung'oa na kubomoa na kuangusha na kuharibu na kudhuru,[h] ndivyo nitakavyokuwa macho kuwaelekea ili kujenga na kupanda,"[i] asema Yehova. **29** "Katika siku hizo hawatasema tena, 'Akina baba ndio waliokula zabibu mbichi, lakini meno ya wana ndiyo yaliyotiwa ukakasi.'[j] **30** Lakini kila mmoja atakufa kwa sababu ya kosa lake mwenyewe.[k] Mtu yeyote atakayekula zabibu mbichi, meno yake ndiyo yatakayotiwa ukakasi."

31 "Tazama! Siku zinakuja," asema Yehova, "nami nitafanya agano jipya[l] pamoja na

nyumba ya Israeli[a] na nyumba
ya Yuda;[b] **32** si kama lile aga-
no ambalo nilifanya pamoja na
mababu zao katika ile siku ni-
lipowashika mkono na kuwa-
toa katika nchi ya Misri,[c] 'aga-
no langu ambalo wao walilivu-
nja,[d] ingawa mimi mwenyewe
nilikuwa mume kwao,'[e] asema
Yehova."

33 "Kwa maana hili ndilo
agano[f] nitakalofanya pamoja
na nyumba ya Israeli baada ya
siku hizo,"[g] asema Yehova. "Ni-
taitia sheria yangu ndani yao,[h]
nami nitaiandika katika moyo
wao.[i] Nami nitakuwa Mungu
wao, nao watakuwa watu wa-
ngu."[j]

34 "Nao hawatafundishana
tena kila mtu na mwenzake
wala kila mtu na ndugu yake,[k]
wakisema, 'Mjueni Yehova!'[l]
kwa maana wote watanijua
mimi, kuanzia yule aliye mdo-
go zaidi kati yao mpaka yule
aliye mkubwa zaidi kati yao,"[m]
asema Yehova. "Kwa maana ni-
talisamehe kosa lao, na dhambi
yao sitaikumbuka tena."[n]

35 Yehova, Mpaji wa jua
kwa ajili ya nuru wakati wa
mchana,[o] sheria[p] za mwezi[q]
na nyota kwa ajili ya nuru wa-
kati wa usiku,[r] Yeye anayei-
chafua bahari ili mawimbi
yake yawe na mchafuko,[s] Yeye
ambaye jina lake ni Yehova
wa majeshi,[t] amesema hivi:
36 "'Kama masharti haya ya-
ngeweza kuondolewa mbele za-
ngu,'[u] asema Yehova, 'vivyo hi-
vyo wale ambao ni uzao wa
Israeli wangeweza kukoma wa-
siwe taifa mbele zangu siku-
zote.'"[v]

37 Yehova amesema hivi:
"'Mbingu zilizo juu zikiweza
kupimwa na misingi ya dunia
iliyo chini ikiweza kuchungu-
zwa,[a] vivyo hivyo mimi mwe-
nyewe ningeweza kuukataa
uzao wote wa Israeli kwa sa-
babu ya yote ambayo wamefa-
nya,'[b] asema Yehova."

38 "Tazama! Siku zinakuja,"
asema Yehova, "na hakika jiji
litajengwa[c] kwa ajili ya Yeho-
va kutoka Mnara wa Hanane-
li[d] mpaka Lango la Pembeni.[e]
39 Na bado kamba ya kupimia[f]
itaenda mbele moja kwa moja
kwenye kilima cha Garebu,
nayo hakika itazunguka mpa-
ka Goa. **40** Na nchi tamba-
rare yote ya chini ya mizoga[g]
na ya majivu yenye mafuta,[h]
na matuta yote mpaka bonde
la mto la Kidroni,[i] mpaka kwe-
nye pembe ya Lango la Fara-
si[j] kuelekea mashariki, itaku-
wa kitu kitakatifu kwa Yeho-
va.[k] Haitang'olewa, wala haita-
bomolewa tena mpaka wakati
usio na kipimo."[l]

32 Neno lililomjia Yeremia
kutoka kwa Yehova ka-
tika mwaka wa kumi wa Se-
dekia mfalme wa Yuda,[m] yaa-
ni, mwaka wa kumi na nane wa
Nebukadreza.[n] **2** Na wakati
huo majeshi ya mfalme wa Ba-
biloni yalikuwa yanazingira Ye-
rusalemu;[o] naye Yeremia nabii
alikuwa chini ya kizuizi kati-
ka Ua wa Walinzi[p] ulio katika
nyumba ya mfalme wa Yuda;
3 kwa sababu Sedekia mfalme
wa Yuda alikuwa amemzuilia,[q]
akisema:

"Kwa nini unatoa unabii,[r]
ukisema, 'Yehova amesema
hivi: "Tazama, ninalitia jiji hili
mkononi mwa mfalme wa Ba-

SURA 31

a Ga 6:16
b Yer 50:4
c Kut 19:5
Kum 1:31
d Eze 16:59
Ebr 8:9
e Yer 3:14
f Ebr 8:6
g Ebr 8:10
h Eze 11:19
Eze 36:26
i Zb 37:31
Ebr 10:16
j Yer 30:22
Ebr 8:10
k Isa 54:13
Yoh 6:45
1Th 4:9
1Yo 2:27
l 1Nya 28:9
Yoh 17:3
m Isa 11:9
Yer 24:7
Hab 2:14
Ebr 8:11
n Yer 33:8
Yer 50:20
Mik 7:18
Mt 26:28
Ro 11:27
Ebr 8:12
Ebr 9:15
Ebr 10:17
o Mwa 1:16
Zb 136:8
Mt 5:45
p 1Ko 14:33
q Ayu 38:33
Zb 89:37
Zb 104:19
r Zb 136:9
s Isa 51:15
t Yer 10:16
u Zb 148:6
Isa 54:10
Yer 33:20
v Zb 72:5

Safu ya 2

a Ayu 38:5
Met 30:4
Isa 40:12
b Yer 30:11
c Ne 12:27
Isa 44:28
Yer 30:18
d Ne 3:1
Ne 12:39
Zek 14:10
e 2Nya 26:9
f Zek 1:16
g Yer 19:11
h Yer 7:32
i 2Sa 15:23
2Fa 23:6
Yoh 18:1
j 2Fa 11:16
2Nya 23:15
Ne 3:28
k Eze 45:1
Yoe 3:17
l Isa 51:22

SURA 32

m 2Fa 25:1
Yer 39:1
n Yer 25:1
o Yer 52:4

p Ne 3:25; Yer 33:1; Yer 37:21; Yer 38:28; q Yer 37:18; Ebr 11:36; r Lu 20:2.

biloni, na hakika yeye atalite-
ka;[a] **4** na Sedekia mwenye-
we, mfalme wa Yuda, hatapo-
nyoka kutoka mkononi mwa
Wakaldayo, kwa maana bila
shaka atatiwa mkononi mwa
mfalme wa Babiloni, na ki-
nywa chake kitasema na ki-
nywa cha yule, na macho yake
yatayaona macho ya yule"';[b]
5 'naye atampeleka Sedekia
mpaka Babiloni, naye ataende-
lea kuwa huko mpaka nitaka-
pomkazia fikira,'[c] asema Yeho-
va; 'ingawa ninyi mnaendelea
kupigana na Wakaldayo, ha-
mtafanikiwa'?"[d]

6 Na Yeremia akasema:
"Neno la Yehova limenijia, na
kusema, **7** 'Tazama, Hana-
meli mwana wa Shalumu ndu-
gu ya baba yako anakuja kwa-
ko, kusema: "Jinunulie shamba
langu lililoko Anathothi,[e] kwa
sababu haki ya kukomboa ni
yako, ulinunue."'"[f]

8 Baada ya muda Hanameli
mwana wa ndugu ya baba ya-
ngu akaingia kwangu, kulinga-
na na lile neno la Yehova, ndani
ya Ua wa Walinzi,[g] naye akani-
ambia: "Tafadhali, nunua sha-
mba langu lililoko Anathothi,[h]
lililo katika nchi ya Benyami-
ni,[i] kwa maana haki ya fungu
la urithi ni yako, na mamlaka
ya kukomboa ni yako. Linunue
liwe lako." Ndipo nikajua kwa-
mba hilo lililokuwa neno la Ye-
hova.[j]

9 Kwa hiyo nikanunua lile
shamba lililoko Anathothi[k] ku-
toka kwa Hanameli[l] mwana wa
ndugu ya baba yangu. Nami ni-
kaanza kumpimia pesa,[m] she-
keli saba na vipande kumi vya
fedha. **10** Kisha nikaandika
katika hati[a] na kutia muhuri[b]
na kuchukua mashahidi[c] nili-
pokuwa nikipima[d] pesa katika
mizani. **11** Baada ya hayo ni-
kachukua ile hati ya ununuzi,
ile iliyotiwa muhuri kulingana
na amri na masharti,[e] na ile ili-
yoachwa wazi; **12** kisha nika-
mpa hati ya ununuzi Baruku[f]
mwana wa Neria[g] mwana wa
Mahseya mbele ya macho ya
Hanameli mwana wa ndugu ya
baba yangu na mbele ya macho
ya mashahidi, wale wenye kua-
ndika katika ile hati ya ununu-
zi,[h] mbele ya macho ya Waya-
hudi wote waliokuwa wameke-
ti katika Ua wa Walinzi.[i]

13 Sasa nikamwamuru Ba-
ruku mbele ya macho yao, ni-
kisema: **14** "Yehova wa maje-
shi, Mungu wa Israeli, amese-
ma hivi, 'Chukua hizi hati, hii
hati ya ununuzi, iliyotiwa mu-
huri, na ile hati nyingine iliyoa-
chwa wazi,[j] nawe uziweke kati-
ka chombo cha udongo, ili zidu-
mu kwa siku nyingi.' **15** Kwa
maana Yehova wa majeshi, Mu-
ngu wa Israeli, amesema hivi,
'Bado nyumba na mashamba
na mizabibu zitanunuliwa kati-
ka nchi hii.'"[k]

16 Nami nikaanza kusali[l]
kwa Yehova baada ya ku-
mpa Baruku[m] mwana wa Ne-
ria[n] ile hati ya ununuzi, nikise-
ma: **17** "Ole wangu, Ee Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yeho-
va![o] Tazama, wewe mwenyewe
umeziumba mbingu na dunia
kwa nguvu zako kuu[p] na kwa
mkono wako ulionyooshwa.[q]
Jambo hilo lote si la ajabu
mno kwako,[r] **18** Wewe una-
yeonyesha fadhili zenye upe-
ndo kuelekea maelfu,[s] na

SURA 32
a Yer 34:2
Yer 37:8
b 2Fa 25:6
Yer 34:3
Yer 37:17
Yer 38:18
Yer 39:5
Yer 52:9
Eze 12:13
c Yer 27:22
d Met 21:30
Yer 21:4
Yer 33:5
Eze 17:15
e Yos 21:18
Yer 1:1
f Law 25:24
Ru 4:4
g Ne 3:25
Yer 37:21
h 1Fa 2:26
1Nya 6:60
i Yos 18:28
j Yer 32:25
k Yer 1:1
l Yer 32:7
m Mwa 23:16

Safu ya 2
a Yer 32:44
b Ne 10:1
c Ru 4:9
Isa 8:2
d Mwa 23:16
e Law 25:15
f Yer 36:4
Yer 36:26
g Yer 51:59
h Yer 32:44
i Ne 3:25
Yer 33:1
j Yer 32:11
Yer 32:44
k Amo 9:14
Zek 3:10
l Flp 4:6
m Yer 32:12
n Yer 51:59
o Yer 1:6
p Mwa 1:1
2Fa 19:15
Zb 102:25
Isa 40:26
Yer 10:12
Ufu 4:11
q 1Fa 8:42
Yer 27:5
r Mwa 18:14
Ayu 42:2
Lu 1:37
Ro 4:21
s Kut 20:6
Kut 34:7

kulipa kosa la akina baba katika vifua vya wana wao baada yao,[a] Mungu wa kweli, aliye Mkuu,[b] Mwenye nguvu,[c] Yehova wa majeshi[d] ndilo jina lake,[e] **19** mkuu katika shauri[f] na mwingi katika matendo,[g] wewe ambaye macho yako yamefunguliwa juu ya njia zote za wanadamu,[h] ili kumpa kila mmoja kulingana na njia zake na kulingana na matunda ya matendo yake;[i] **20** wewe uliyeweka ishara na miujiza katika nchi ya Misri mpaka leo hii na katika Israeli na kati ya wanadamu,[j] ili ujifanyie jina, kama ilivyo leo hii.[k] **21** Nawe ukawatoa watu wako Israeli katika nchi ya Misri,[l] kwa ishara na kwa miujiza[m] na kwa mkono wenye nguvu na kwa mkono ulionyooshwa na kwa hali kuu ya kuogopesha.[n]

22 "Baada ya muda ukawapa nchi hii ambayo uliwaapia mababu zao kuwapa,[o] nchi inayotiririka maziwa na asali.[p] **23** Nao wakaingia na kuimiliki,[q] lakini hawakuitii sauti yako, nao hawakutembea katika sheria yako.[r] Mambo yote uliyowaamuru kufanya hawakuyafanya,[s] hivi kwamba ukafanya msiba huu wote uwangukie.[t] **24** Tazama! Watu wamekuja na maboma ya kuzingira[u] kwenye jiji ili kuliteka,[v] na jiji hili hakika litatiwa mkononi mwa Wakaldayo wanaopiga vita juu yake,[w] kwa sababu ya upanga[x] na njaa[y] na tauni;[z] na lile ulilosema limetendeka, na, tazama, wewe unaliona.[a] **25** Ingawa wewe mwenyewe umeniambia, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'Jinunulie lile shamba kwa pesa[a] na kuchukua mashahidi,'[b] ingawa lazima jiji lenyewe litatiwa mkononi mwa Wakaldayo."[c]

26 Ndipo neno la Yehova likamjia Yeremia, na kusema: **27** "Mimi hapa, Yehova, Mungu wa wote wenye mwili.[d] Je, kwangu mimi kuna jambo lolote ambalo ni la ajabu mno?[e] **28** Kwa hiyo Yehova amesema hivi, 'Tazama, ninalitia jiji hili katika mkono wa Wakaldayo na katika mkono wa Nebukadreza mfalme wa Babiloni, naye lazima ataliteka.[f] **29** Na Wakaldayo wanaopiga vita juu ya jiji hili watainga ndani na kuliwasha jiji hili na kuliteketeza kwa moto[g] na nyumba ambazo juu ya paa zake wamemfukizia Baali moshi wa dhabihu na kuimiminia miungu mingine matoleo ya kinywaji kwa kusudi la kunitia uchungu.'[h]

30 "'Kwa maana wana wa Israeli na wana wa Yuda wamekuwa tu watendaji wa mambo mabaya machoni pangu, tangu ujana wao na kuendelea;[i] kwa maana wana wa Israeli pia wananitia uchungu kwa kazi za mikono yao,'[j] asema Yehova. **31** 'Kwa maana jiji hili, tangu siku walipolijenga, mpaka leo hii, limekuwa tu kisababishi cha hasira ndani yangu[k] na kisababishi cha ghadhabu ndani yangu, ili kuliondoa mbele za uso wangu,[l] **32** kwa sababu ya ubaya wote wa wana wa Israeli[m] na wa wana wa

SURA 32

a Hes 14:18
Kum 5:9
1Fa 14:10
Isa 65:6
b Ne 1:5
c Kum 10:17
Isa 10:21
d Zb 148:2
e Yer 10:16
f Isa 28:29
g Kut 15:11
h 2Nya 16:9
Ayu 34:21
Zb 33:13
Zb 66:7
Met 5:21
Met 15:3
Ebr 4:13
i Kut 34:7
Zb 62:12
Mhu 12:14
Yer 17:10
Mt 12:36
Ro 2:6
j Kut 7:3
Kum 4:34
Ne 9:10
Zb 78:43
k Kut 9:16
2Sa 7:23
Isa 63:12
Da 9:15
Ro 9:17
l Kut 6:6
Kut 13:14
m Zb 105:27
Zb 106:9
n Kut 6:1
Kut 15:16
Kum 26:8
1Nya 17:21
Zb 136:12
o Mwa 13:15
Mwa 17:8
Mwa 26:3
Kum 1:8
p Kut 3:8
Yer 11:5
q Ne 9:23
Zb 105:44
r Ne 9:26
Da 9:10
s Hes 33:52
t Kum 28:15
Yos 23:16
Ezr 9:7
u Kum 28:52
Yer 33:4
Eze 4:2
v Law 26:31
2Fa 25:1
Yer 52:4
w Yer 21:4
x Law 26:33
Yer 14:12
y Kum 28:57
Yer 15:2
z Kum 28:59
Yer 24:10
a Isa 55:11

Safu ya 2

a Law 27:18
b Kum 19:15
Mt 18:16
c Yer 37:10
d Hes 16:22
Hes 27:16
Lu 3:6
Ro 3:29
e Mwa 18:14
Ayu 42:2
Lu 1:37
Ro 4:21
f 2Fa 25:4
Yer 20:5
Yer 21:4

g 2Fa 25:9; 2Nya 36:19; Yer 37:8; Yer 52:13; Omb 4:11; h 2Fa 17:16; 2Nya 28:2; Yer 7:18; Yer 19:13; Yer 44:25; i Kum 9:7; 2Fa 17:9; Ne 9:16; Zb 106:6; Yer 2:7; Yer 3:25; Eze 16:8; Eze 20:28; Mdo 7:51; j Yer 22:21; Eze 23:3; k 1Fa 11:7; 2Fa 21:4; Sef 3:1; l 2Fa 23:27; 2Fa 24:3; Omb 1:8; m 2Fa 15:18; 2Fa 17:11; 2Fa 17:18; Yer 7:12; Yer 11:17.

Yuda[a] ambao wametenda ili
kunitia uchungu,[b] wao, wafa-
lme[c] wao, wakuu[d] wao, maku-
hani[e] wao na manabii[f] wao, na
watu wa Yuda na wakaaji wa
Yerusalemu. **33** Nao wakae-
ndelea kunipa mimi mgongo
wala si uso;[g] ingawa walikuwa
wakifundishwa, kuamka ma-
pema na kuwafundisha, laki-
ni hakuna hata mmoja wao
aliyesikiliza ili kupokea ni-
dhamu.[h] **34** Nao wakawa wa-
kiweka machukizo yao katika
nyumba ambayo jina langu li-
meitwa juu yake, ili kuitia una-
jisi.[i] **35** Na zaidi ya hayo, wa-
lijenga mahali pa juu pa Baali[j]
palipo katika bonde la mwana
wa Hinomu,[k] ili kuwapitisha
wana wao na binti zao moto-
ni[l] kwa Moleki,[m] jambo amba-
lo sikuwaamuru,[n] wala hali-
kuingia moyoni mwangu kufa-
nya chukizo hili,[o] kwa kusudi
la kufanya Yuda watende dha-
mbi.'[p]

36 "Na sasa, basi, Yehova
Mungu wa Israeli amesema
hivi kuhusu jiji hili ambalo ni-
nyi mnasema hakika litatiwa
mkononi mwa mfalme wa Ba-
biloni kwa upanga na kwa njaa
na kwa tauni,[q] **37** 'Tazama,
ninawakusanya pamoja kuto-
ka katika nchi zote ambako ni-
takuwa nimewatawanya kati-
ka hasira yangu na katika gha-
dhabu yangu na katika hasi-
ra kuu;[r] nami nitawarudisha
mahali hapa na kuwakalisha
katika usalama.[s] **38** Na haki-
ka wao watakuwa watu wa-
ngu,[t] nami mwenyewe nita-
kuwa Mungu wao.[u] **39** Nami
nitawapa moyo mmoja[v] na
njia moja ili waniogope siku-
zote, iwe kwa mema yao na
kwa mema ya wana wao ba-
ada yao.[a] **40** Nami nitafanya
pamoja nao agano linalodumu
mpaka wakati usio na kipimo,[b]
kwamba mimi sitageuka kuto-
ka nyuma yao, ili niwatendee
mema;[c] nami nitatia ndani ya
moyo wao hali ya kuniogopa
mimi ili wasigeuke kando ku-
toka kwangu.[d] **41** Nami nita-
furahi juu yao ili niwatendee
mema,[e] nami nitawapanda ka-
tika nchi hii[f] katika ukweli
kwa moyo wangu wote na kwa
nafsi yangu yote.'"

42 "Kwa maana Yehova
amesema hivi, 'Kama nilivyole-
ta huu msiba wote mkubwa
juu ya watu hawa, ndivyo nita-
kavyoleta juu yao wema wote
ambao ninasema kuwahusu.[g]
43 Na hakika mashamba ya-
tanunuliwa katika nchi hii[h]
ambayo ninyi mtakuwa mki-
sema: "Hiyo ni mahame yenye
ukiwa[i] yasiyo na mwanada-
mu wala mnyama wa kufugwa.
Imetiwa mkononi mwa Waka-
ldayo."'[j]

44 "'Watu watanunua ma-
shamba kwa pesa, na maandi-
shi yatatiwa katika hati[k] na
muhuri kutiwa na mashahidi[l]
kuchukuliwa, katika nchi ya
Benyamini,[m] na katika maeneo
yanayozunguka Yerusalemu,[n]
na katika majiji ya Yuda,[o] na
katika majiji ya eneo lenye mi-
lima, na katika majiji ya nchi
tambarare ya chini,[p] na katika
majiji ya kusini,[q] kwa sababu
nitawarudisha mateka wao,'[r]
asema Yehova."

SURA 32

a Yer 5:11
Yer 11:10
Eze 8:17
b Isa 1:4
c 1Fa 11:9
2Fa 23:26
1Nya 10:13
Ezr 9:7
Yer 15:4
d Eze 22:6
Da 9:8
e Ne 9:34
f Mik 3:5
Mik 3:11
g 2Nya 29:6
Yer 2:27
Yer 7:24
Zek 7:11
h 2Nya 36:16
Yer 7:13
Yer 25:3
Yer 26:5
Yer 35:15
Yer 44:5
i 2Fa 21:4
2Nya 33:4
Yer 7:30
Yer 23:11
Eze 5:11
Eze 8:5
Eze 23:38
Ho 9:10
j 1Fa 11:5
2Fa 23:10
k Yos 15:8
2Nya 28:3
Yer 19:5
l 2Nya 33:6
Isa 57:5
Yer 7:31
m Law 18:21
Law 20:4
n Kum 18:10
1Fa 11:10
o 1Fa 11:33
p 2Fa 16:3
2Nya 33:9
q Yer 24:10
r Kum 29:24
Kum 30:3
Yer 23:3
Yer 29:14
Eze 37:21
s Yer 23:6
Yer 33:16
Eze 34:25
t Yer 24:7
Yer 31:33
Mik 4:5
u Mwa 17:7
Yer 30:22
v 2Nya 30:12
Eze 11:19

Safu ya 2

a Kum 5:29
Zb 115:13
b Isa 55:3
Isa 61:8
c Zb 73:1
Zb 125:4
Eze 39:29
d Eze 36:26
Ufu 15:4
e Kum 30:9
Isa 62:5
Isa 65:19
Sef 3:17
f Isa 58:11
Isa 61:3
Yer 24:6
Yer 31:12
Amo 9:15
g Yer 31:28
Yer 33:11
Zek 8:15
h Eze 37:14

i Yer 9:11; Eze 23:33; j Yer 21:4; k Yer 32:10; l Yer 32:25; m Yos 18:28; n Yer 33:16; o Yer 31:23; p Yos 15:33; Yer 17:26; Yer 33:13; q Yos 15:21; r Zb 126:1; Yer 33:7.

33 Na neno la Yehova likamjia Yeremia mara ya
pili, alipokuwa bado amefungiwa katika Ua wa Walinzi,[a] likisema: **2** "Yehova, Mtengenezaji[b] wa dunia, amesema hivi,
Yehova Mfanyizaji[c] wake ili kuifanya imara,[d] Yehova ndilo
jina lake,[e] **3** 'Niite, nami nitakujibu na kukuambia kwa
utayari[f] mambo makubwa na yasiyoweza kueleweka, usiyo-
yajua.'"[g]
4 "Kwa maana Yehova Mungu wa Israeli amesema hivi
kuhusu nyumba za jiji hili na kuhusu nyumba za wafalme wa
Yuda ambazo zimebomolewa kwa sababu ya maboma ya ku-
zingira na kwa sababu ya upanga;[h] **5** kuhusu wale wanaokuja kupiga vita juu ya Wa-
kaldayo na kujaza mahali pengi kwa mizoga ya watu
ambao nimewapiga na kuwaua katika hasira yangu na ka-
tika ghadhabu yangu,[i] na kwa sababu ya wote ambao kuto-
kana na ubaya wao nimeficha uso wangu kutoka kwe-
nye jiji hili,[j] **6** 'Tazama, ninamletea yeye nguvu na
afya;[k] nami nitawaponya na kuwafunulia wingi wa amani
na kweli.[l] **7** Nami nitawarudisha mateka wa Yuda na ma-
teka wa Israeli,[m] nami nitawajenga kama pale mwanzoni.[n]
8 Nami nitawatakasa kutoka katika kosa lao lote ambalo ku-
pitia hilo wamenitendea dhambi,[o] nami nitayasamehe ma-
kosa yao yote ambayo kupitia hayo wamenitendea dha-
mbi na ambayo kupitia hayo wamenikosea.[p] **9** Na hakika
yeye atakuwa kwangu jina la furaha,[q] sifa na uzuri kuelekea
mataifa yote ya dunia ambayo yatasikia ule wema wote
ambao ninawapa.[a] Na hakika
wao watakuwa na hofu[b] na ku-
fadhaika[c] kwa sababu ya ule
wema wote na kwa sababu ya
ile amani yote ambayo nina-
mpa.'"[d]
10 "Yehova amesema hivi,
'Katika mahali hapa ambapo ninyi mtakuwa mkise-
ma ni ukiwa usio na mwanadamu wala mnyama wa kufu-
gwa, katika majiji ya Yuda na katika barabara za Yerusale-
mu ambazo ziko ukiwa[e] pasipo na mwanadamu wala mka-
aji wala mnyama wa kufugwa, bado itasikiwa[f] **11** sauti ya
furaha na sauti ya shangwe,[g] sauti ya bwana-arusi na sauti
ya bibi-arusi, sauti ya wale wanaosema: "Msifuni Yehova wa
majeshi, kwa maana Yehova ni mwema;[h] kwa maana fadhili
zake zenye upendo ni za mpaka wakati usio na kipimo!"'[i]
"'Watakuwa wakileta toleo
la shukrani katika nyumba ya
Yehova,[j] kwa maana nitawa-
rudisha mateka wa nchi kama
pale mwanzoni,'[k] Yehova ame-
sema."
12 "Yehova wa majeshi ame-
sema hivi, 'Katika mahali hapa
palipo ukiwa bila mwanadamu
na hata mnyama wa kufugwa[l]
na katika majiji yake yote bado
patakuwa na uwanja wa malis-
ho wa wachungaji wanaolilaza
kundi.'[m]
13 "'Katika majiji ya eneo
lenye milima, katika majiji ya
nchi ya chini,[n] na katika ma-
jiji ya kusini,[o] na katika nchi
ya Benyamini,[p] na katika ma-

SURA 33

a Ne 3:25
Yer 32:2
Yer 37:21
Yer 38:28
b Mwa 1:1
Zb 146:6
Ufu 4:11
c Mwa 14:19
Zb 102:25
Isa 45:18
Ufu 10:6
d Zb 96:10
Zb 104:5
Zb 119:90
Mhu 1:4
e Kut 6:3
Kut 15:3
Yer 32:18
Amo 5:8
Amo 9:6
f Kum 4:7
Zb 50:15
Zb 91:15
Isa 55:6
Yer 29:12
g Zb 25:14
Isa 48:6
Amo 3:7
h Kum 28:52
Yer 32:24
i Yer 32:5
j Kum 31:17
Yer 21:10
Mik 3:4
k Kum 32:39
Isa 30:26
Yer 30:17
l Isa 54:13
m Kum 30:3
Zb 14:7
Yer 30:3
Yer 32:44
n Isa 1:26
Yer 24:6
Zek 10:6
o Zb 85:2
Isa 40:2
Yer 31:34
Zek 13:1
p Zb 65:3
Isa 43:25
Isa 44:22
Mik 7:18
q Kum 30:9
Zb 126:3
Isa 62:3

Safu ya 2

a Isa 62:7
b 2Nya 20:29
c Mik 7:17
d Ne 6:16
e Isa 24:11
f Yer 32:43
g Yer 31:12
h Zb 25:8
Zek 9:17
Mk 10:18
i 1Nya 16:8
2Nya 5:13
Ezr 3:11
Zb 89:2
Isa 12:4
Mik 7:18
j Law 7:12
2Nya 29:31
Zb 107:22
k Kum 30:5
Yer 32:44
l Yer 32:43
Yer 51:62
m Isa 65:10
Yer 31:24
Yer 50:19
Mik 2:12
n Yos 15:33
Yer 32:44

o Yos 15:21; p Yos 18:21.

zingira ya Yerusalemu,[a] na katika majiji ya Yuda,[b] bado makundi yatapita chini ya mikono ya mtu anayehesabu,'[c] Yehova amesema."

14 "'Tazama! Siku zinakuja,'[d] asema Yehova, 'na hakika mimi nitalitimiza neno jema ambalo nimesema,[e] kuihusu nyumba ya Israeli[f] na kuihusu nyumba ya Yuda. **15** Katika siku hizo na katika wakati huo nitamchipushia Daudi chipukizi la uadilifu,[g] na hakika yeye atatenda haki na uadilifu katika nchi.[h] **16** Katika siku hizo Yuda ataokolewa[i] na Yerusalemu litakaa katika usalama.[j] Naye ataitwa hivi, Yehova Ni Uadilifu Wetu.'"[k]

17 "Kwa maana Yehova amesema hivi, 'Hatakatiliwa mbali, kuhusu Daudi, mwanamume wa kuketi juu ya kiti cha ufalme cha nyumba ya Israeli.[l] **18** Nao makuhani Walawi, hatakatiliwa mbali mwanamume kutoka mbele zangu wa kutoa toleo zima la kuteketezwa na kufukiza moshi pamoja na toleo la nafaka na kutoa dhabihu sikuzote.'"[m]

19 Na neno la Yehova likaendelea kumjia Yeremia, na kusema: **20** "Yehova amesema hivi, 'Ikiwa ninyi mnaweza kulivunja agano langu la mchana na agano langu la usiku, ili mchana na usiku usije kwa wakati wake,[n] **21** vivyo hivyo agano langu linaweza kuvunjwa pamoja na Daudi mtumishi wangu[o] ili asiwe na mwana anayetawala akiwa mfalme juu ya kiti chake cha ufalme;[p] pia pamoja na makuhani, Walawi, wahudumu wangu.[q] **22** Kama jeshi la mbinguni lisivyoweza kuhesabiwa, wala mchanga wa bahari kupimwa,[a] ndivyo nitakavyouzidisha uzao wa Daudi mtumishi wangu na Walawi wanaonihudumia.'"[b]

23 Na neno la Yehova likaendelea kumjia Yeremia, na kusema: **24** "Je, hujaona yale ambayo watu wa kikundi hiki wamesema, 'Zile familia mbili ambazo Yehova amechagua,[c] yeye pia atazikataa'? Nao wanaendelea kuwavunjia watu wangu heshima,[d] hivi kwamba lisiendelee tena kuwa taifa mbele yao.

25 "Yehova amesema hivi, 'Kama haingekuwa kweli kwamba nilikuwa nimeliweka agano langu la mchana na usiku,[e] sheria za mbingu na dunia,[f] **26** vivyo hivyo pia ningeukataa uzao wa Yakobo na wa Daudi mtumishi wangu,[g] ili nisichukue kutoka kwa uzao wake watawala kuwa juu ya uzao wa Abrahamu, Isaka na Yakobo. Kwa maana nitawakusanya mateka[h] wao nami nitawahurumia.'"[i]

34 Neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova, wakati Nebukadreza mfalme wa Babiloni[j] na jeshi lake lote[k] na falme zote za dunia, mamlaka iliyo chini ya mkono wake,[l] na vikundi vyote vya watu vilipokuwa vikipiga vita juu ya Yerusalemu na juu ya majiji yake yote,[m] kusema:

2 "Yehova Mungu wa Israeli amesema hivi, 'Nenda, umwambie Sedekia mfalme wa Yuda,[n] ndiyo, umwambie hivi: "Yehova amesema hivi, 'Tazama, ninalitia jiji hili mkononi mwa mfalme wa Babiloni,[o]

SURA 33

a Yer 17:26
b Yer 32:44
c Law 27:32
d Yer 23:5
e Mwa 22:17
Kum 30:3
Yer 29:10
f Yer 31:27
g 1Nya 17:11
Isa 4:2
Isa 11:1
Isa 53:2
Yer 23:5
Zek 3:8
Zek 6:12
Ufu 22:16
h Isa 9:7
Isa 11:4
Ebr 1:9
i Isa 45:17
j Kum 33:28
Eze 28:26
k Yer 23:6
l 2Sa 7:16
1Fa 2:4
Zb 89:29
Isa 9:7
Lu 1:33
m 1Pe 2:5
Ufu 1:6
n Mwa 1:16
Zb 89:37
Isa 54:10
Yer 31:35
o 2Sa 7:16
2Sa 23:5
Zb 89:34
Zb 132:11
Isa 55:3
Yer 31:37
p Isa 9:6
Da 7:14
Lu 1:32
q Kum 21:5

Safu ya 2

a Mwa 13:16
Mwa 15:5
Mwa 22:17
Yer 31:37
Ebr 11:12
b 1Nya 25:1
2Nya 35:2
c Eze 37:19
d Zb 83:4
Eze 25:3
e Mwa 1:16
Yer 33:20
f Ayu 38:33
Zb 74:16
Zb 104:19
Yer 31:35
g Zb 94:14
Yer 31:37
h Ezr 2:1
Ezr 2:70
Yer 33:7
i Isa 14:1
Yer 31:20
Ho 1:7
Mik 7:19
Zek 10:6

SURA 34

j 2Fa 25:1
Yer 32:2
k Yer 39:1
Yer 52:4
l Yer 27:6
m Kum 28:52
Yer 1:15
n 2Nya 36:11
Yer 37:1
o Yer 21:10
Yer 32:28

naye ataliteketeza kwa moto.[a]
3 Nawe mwenyewe hutaponyoka kutoka mkononi mwake, kwa sababu bila shaka utakamatwa na kutiwa mkononi mwake.[b] Na macho yako yatayaona macho ya mfalme wa Babiloni,[c] na kinywa chake kitasema na kinywa chako, nawe utaenda Babiloni.' **4** Hata hivyo, lisikie neno la Yehova, Ee Sedekia mfalme wa Yuda,[d] 'Yehova amesema hivi kukuhusu wewe: "Hutakufa kwa upanga. **5** Utakufa kwa amani;[e] nao watakufanyia mfukizo,[f] kama ule mfukizo ambao waliwafanyia baba zako, wale wafalme wa zamani waliokutangulia,[g] na 'Aa, Ee bwana!'[h] ndivyo watakavyosema wakikuombolezea,[i] kwa maana 'mimi mwenyewe nimesema neno hili,' asema Yehova."'"'"

6 Na Yeremia nabii akamwambia Sedekia mfalme wa Yuda maneno hayo yote[j] katika Yerusalemu, **7** wakati majeshi ya mfalme wa Babiloni yalipokuwa yakipiga vita juu ya Yerusalemu na juu ya majiji yote ya Yuda ambayo yalikuwa yamebaki,[k] juu ya Lakishi[l] na juu ya Azeka;[m] kwa maana hayo, majiji yenye ngome,[n] ndiyo yaliyobaki kati ya majiji ya Yuda.[o]

8 Neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova baada ya Mfalme Sedekia kufanya agano pamoja na watu wote waliokuwa Yerusalemu ili kuwatangazia uhuru,[p] **9** kila mtu kumwachilia huru mtumishi wake wa kiume na kila mtu mjakazi wake, mwanamume Mwebrania[q] na mwanamke Mwebrania, ili wasiwatumie kama watumishi, yaani, Myahudi, ambaye ni ndugu yake.[a]
10 Basi wakuu[b] wote wakatii, na watu wote waliokuwa wameingia katika agano la kwamba kila mtu amwachilie huru mtumishi wake wa kiume na kila mtu mjakazi wake, ili wasiwatumie tena kama watumishi, nao wakatii na kuwaachilia waende zao.[c] **11** Lakini wakageuka[d] baada ya hayo na kuanza kuwarudisha wale watumishi wa kiume na wajakazi ambao walikuwa wamewaachilia huru, nao wakawatiisha kama watumishi wa kiume na kama wajakazi.[e] **12** Kwa hiyo neno la Yehova likamjia Yeremia kutoka kwa Yehova, na kusema:

13 "Yehova Mungu wa Israeli amesema hivi, 'Mimi mwenyewe nilifanya agano pamoja na mababu[f] zenu katika siku ile nilipowatoa katika nchi ya Misri,[g] kutoka katika nyumba ya watumishi,[h] nikisema: **14** "Mwishoni mwa miaka saba mnapaswa kumwachilia kila mtu ndugu yake,[i] Mwebrania,[j] ambaye uliuziwa[k] na ambaye amekutumikia miaka sita; nawe lazima umwachilie aende huru asiwe pamoja nawe." Lakini mababu zenu hawakunisikiliza, wala hawakutega sikio lao.[l] **15** Nanyi leo mnageuka na kufanya yaliyo sawa machoni pangu kwa kumtangazia uhuru kila mtu mwenzake, nanyi mnafanya agano mbele zangu[m] ndani ya nyumba ambayo jina langu limeitwa juu yake.[n] **16** Kisha mnageuka[o] nyuma na kulitia unajisi jina langu[p] na kumrudisha kila mtu mtumishi wake wa kiume na kila mtu mja-

SURA 34

a Yer 32:29
Yer 37:8
Yer 38:23
Yer 39:8
b Yer 37:17
Yer 39:5
Yer 52:8
c 2Fa 25:6
Yer 32:4
Eze 12:13
d 2Nya 36:10
e Eze 17:16
f 2Nya 16:14
g 2Nya 21:19
h Yer 22:18
i Omb 4:20
Mik 2:4
j 1Sa 3:18
1Fa 21:19
Mdo 20:27
k Kum 28:52
Yer 4:5
l 2Fa 19:8
Mik 1:13
m Yos 15:35
n 2Fa 18:13
2Nya 11:5
o 2Nya 27:4
p Kut 21:2
Law 25:10
Kum 15:12
q Mwa 14:13
2Ko 11:22

Safu ya 2

a Law 25:39
Ne 5:8
b Yer 26:10
Yer 36:12
c Law 25:39
d Ho 6:4
e Law 25:42
Zb 36:3
f Kut 24:7
Kum 5:2
g Kum 7:8
Kum 24:18
h Kut 13:3
i Kut 21:2
Law 25:41
j Kum 15:12
k Law 25:39
l 1Sa 8:8
2Fa 17:14
Ne 9:29
Yer 7:26
Zek 7:12
m Zb 119:106
n 2Fa 21:4
o Mhu 5:5
Eze 17:16
Mt 5:37
p Law 19:12
Eze 20:39

kazi wake, ambaye mlimwachilia huru kwa kukubaliana na nafsi yao, nanyi mnawatiisha wawe watumishi wenu wa kiume na wajakazi wenu.'[a]

17 "Kwa hiyo Yehova amesema hivi, 'Ninyi hamkunitii mimi kwa kuendelea kumtangazia uhuru[b] kila mtu ndugu yake na kila mtu mwenzake. Tazama, mimi ninawatangazia ninyi uhuru,'[c] asema Yehova, 'upanga,[d] tauni[e] na njaa,[f] na hakika mimi nitawatoa ninyi kwa ajili ya kutetemesha falme zote za dunia.[g] **18** Nami nitawatoa wale watu wanaolivunja agano langu,[h] kwa sababu hawakutenda yale maneno ya agano ambalo walifanya mbele zangu kwa yule ndama ambaye walimkata vipande viwili[i] ili wapite katikati ya vipande vyake;[j] **19** yaani, wakuu wa Yuda na wakuu wa Yerusalemu,[k] maofisa wa makao ya mfalme na makuhani na watu wote wa nchi waliopita katikati ya vile vipande vya ndama— **20** ndiyo, nitawatia mkononi mwa adui zao na mkononi mwa wale wanaoitafuta nafsi yao;[l] na maiti zao zitakuwa chakula kwa viumbe vinavyoruka vya mbinguni na kwa wanyama wa dunia.[m] **21** Na Sedekia mfalme wa Yuda[n] na wakuu wake nitawatia mkononi mwa adui zao na mkononi mwa wale wanaoitafuta nafsi yao na mkononi mwa majeshi ya mfalme wa Babiloni[o] ambayo yanaondoka kuwaacha ninyi.'[p]

22 "'Tazama, mimi ninaamuru,' asema Yehova, 'na hakika mimi nitawarudisha katika jiji hili,[q] nao watapiga vita juu yake na kuliteka na kuliteketeza kwa moto;[a] na majiji ya Yuda nitayafanya kuwa mahame yenye ukiwa bila mkaaji.'"[b]

35 Neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yehova katika siku za Yehoyakimu[c] mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, na kusema: **2** "Nenda katika nyumba ya Warekabu,[d] na useme nao na kuwaleta katika nyumba ya Yehova, katika kimoja cha vyumba vya kulia chakula; nawe uwape divai wanywe."

3 Kwa hiyo nikamchukua Yaazania mwana wa Yeremia mwana wa Habasinia na ndugu zake, na wanawe wote, na nyumba yote ya Warekabu, **4** nami nikawaleta katika nyumba ya Yehova, kwenye chumba cha kulia[e] chakula cha wana wa Hanani mwana wa Igdalia, mtu wa Mungu wa kweli, kilichokuwa kando ya chumba cha kulia chakula cha wakuu ambacho kilikuwa juu ya chumba cha kulia chakula cha Maaseya mwana wa Shalumu[f] mtunza-mlango. **5** Kisha nikatia mbele ya wana wa nyumba ya Warekabu vikombe vilivyojaa divai na bilauri na kuwaambia: "Kunyweni divai."

6 Lakini wakasema: "Sisi hatutakunywa divai, kwa sababu Yonadabu mwana wa Rekabu,[g] babu yetu, ndiye aliyeweka amri juu yetu, akisema, 'Msinywe divai, ninyi wala wana wenu, mpaka wakati usio na kipimo.[h] **7** Nanyi msijenge nyumba, wala msipande mbegu; wala msipande shamba la mizabibu, wala lisije

SURA 34

a Yer 34:11
b Kut 21:2
Law 25:10
Kum 15:12
c Law 26:34
Ga 6:7
Yak 2:13
d Yer 15:2
e Law 26:25
Yer 21:7
Eze 14:19
f Kum 28:53
2Fa 25:3
Yer 24:10
Yer 32:24
g Kum 28:65
Yer 15:4
Yer 29:18
h Kum 17:2
Yos 7:11
Eze 17:16
Ho 6:7
i Mwa 15:10
j Mwa 15:17
k Yer 25:18
Da 9:6
l Kum 7:10
Yer 4:30
m Kum 28:26
1Fa 14:11
Zb 79:2
Yer 7:33
Yer 16:4
Yer 19:7
n 2Fa 24:18
o 2Fa 25:6
Yer 39:6
Yer 52:10
Omb 4:20
p Yer 37:5
q 2Nya 36:17
Yer 39:1

Safu ya 2

a 2Fa 25:9
Yer 32:29
Yer 38:23
Yer 39:8
Yer 52:13
b Law 26:33
Kum 29:28
Yer 9:11
Yer 44:2
Mik 7:13

SURA 35

c 2Fa 23:34
2Nya 36:5
Da 1:1
d 2Fa 10:15
1Nya 2:55
e 2Nya 31:11
f 1Nya 9:17
Ezr 2:42
Ne 7:45
g 2Fa 10:15
1Nya 2:55
h Mhu 5:4

kuwa lenu. Lakini mkae katika mahema siku zenu zote,
ili mwendelee kuishi siku nyingi juu ya uso wa nchi ambapo mnakaa mkiwa wageni.'[a]
8 Kwa hiyo tunaendelea kuitii sauti ya Yehonadabu mwana wa Rekabu babu yetu katika
kila jambo ambalo alituamuru[b] kwa kutokunywa divai yoyote siku zetu zote, sisi, wake
zetu, wana wetu na binti zetu,[c]
9 na kwa kutojenga nyumba za sisi kukaa ndani, hivi kwamba tusije tukawa na mizabibu yoyote wala shamba wala mbegu. **10** Nasi tunaendelea kukaa katika mahema na kutii na kufanya kulingana na
yote ambayo Yonadabu[d] babu yetu alituamuru.[e] **11** Lakini ikawa kwamba Nebukadreza mfalme wa Babiloni alipokuja juu ya nchi[f] tukaanza kusema, 'Njooni, tuingie ndani ya Yerusalemu kwa sababu ya jeshi la Wakaldayo na kwa sababu ya jeshi la Wasiria, nasi tukae Yerusalemu.'"[g]

12 Na neno la Yehova likamjia Yeremia, na kusema:
13 "Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi, 'Nenda, uwaambie watu wa Yuda na wakaaji wa Yerusalemu: "Je, ninyi sikuzote hamkupokea himizo la kuyatii maneno yangu?"[h] asema Yehova.
14 "Maneno ya Yehonadabu mwana wa Rekabu[i] yametimizwa, ambayo aliwaamuru wanawe, wasinywe divai yoyote, nao hawajanywa yoyote mpaka leo hii, kwa sababu wameitii amri ya babu yao.[j] Na kwa habari yangu, nimesema nanyi, nikiamka mapema na kusema,[k] lakini hamkunitii mimi.[l]

SURA 35
a Kut 20:12
Efe 6:3
b Mwa 18:19
c Met 6:20
d 2Fa 10:15
1Nya 2:55
e Yer 35:8
f 2Nya 36:6
Da 1:1
g Yer 4:5
h Kum 5:29
Yer 6:8
Yer 7:3
Yer 9:12
Yer 32:33
i 2Fa 10:15
1Nya 2:55
j Yer 35:8
k 2Nya 36:15
Yer 7:13
Yer 25:3
l Ne 9:26
Ne 9:30
Isa 30:9
Yer 7:24

Safu ya 2
a Yer 7:25
Yer 25:4
b Isa 1:16
Yer 4:14
Yer 25:5
Eze 18:30
Ho 14:1
Zek 1:3
c Yer 7:3
Yer 18:11
d Kum 31:18
Yer 44:5
e Kum 30:20
Yos 14:1
Yer 7:7
f 2Nya 36:16
g 1Nya 2:55
h Yer 35:8
i Isa 1:3
Yer 11:8
j Kum 28:15
Kum 29:27
Yos 23:15
2Fa 23:27
Yer 15:3
Mik 3:12
k Met 1:24
Isa 65:12
Isa 66:4
Yer 7:13
Yer 26:5
Yer 32:33
l 2Fa 10:15
m Kut 20:12
Kum 5:16
n Zb 5:5
Yer 15:19
Lu 21:36
o Efe 6:3
Kol 3:20

SURA 36
p 2Fa 23:36
Yer 25:1

15 Nami niliendelea kutuma kwenu watumishi wangu wote manabii,[a] nikiamka mapema na kuwatuma, na kusema, 'Tafadhali rudini, kila mmoja kutoka katika njia yake mbaya,[b] nanyi fanyeni matendo yenu kuwa mema,[c] wala msiifuate miungu mingine ili kuitumikia.[d] Na mwendelee kukaa katika nchi ambayo nimewapa ninyi na mababu zenu.'[e] Lakini hamkutega sikio lenu, wala hamkunisikiliza.[f] **16** Lakini wana wa Yehonadabu mwana wa Rekabu[g] wameitenda amri ya babu yao ambayo aliwaamuru;[h] lakini watu hawa, hawakunisikiliza mimi."'"[i]

17 "Kwa hiyo Yehova, Mungu wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi, 'Tazama, ninaleta juu ya Yuda na juu ya wakaaji wote wa Yerusalemu ule msiba wote ambao nimesema juu yao,[j] kwa sababu nimesema nao lakini hawakusikiliza, nami niliendelea kuwaita lakini hawakujibu.'"[k]

18 Na Yeremia akawaambia nyumba ya Warekabu: "Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi, 'Kwa sababu mmeitii amri ya Yehonadabu[l] babu yenu nanyi mnaendelea kuzishika amri zake zote na kufanya kulingana na yote ambayo aliwaamuru,[m]
19 basi Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi: "Hatakatiliwa mbali kutoka kwa Yonadabu mtu wa kusimama[n] mbele zangu sikuzote."'"[o]

36 Ikawa kwamba katika mwaka wa nne wa Yehoyakimu[p] mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, neno hili likamjia

Yeremia kutoka kwa Yehova,
likisema: **2** "Chukua kitabu
cha kukunjwa,[a] uandike nda-
ni yake maneno[b] yote amba-
yo nimekuambia juu ya Israeli
na juu ya Yuda[c] na juu ya ma-
taifa yote,[d] tangu siku niliyo-
sema nawe, tangu siku za Yo-
sia, mpaka leo hii.[e] **3** Labda
wale wa nyumba ya Yuda wa-
tausikiliza msiba wote ninaofi-
kiria kuwatendea,[f] kusudi wa-
rudi, kila mmoja kutoka katika
njia yake mbaya,[g] na ili mimi
kwa kweli nisamehe kosa lao
na dhambi yao."[h]

4 Na Yeremia akamwita Ba-
ruku[i] mwana wa Neria ili Baru-
ku aandike kwa kinywa cha Ye-
remia maneno yote ya Yehova
ambayo Yeye alikuwa ame-
mwambia, katika kile kitabu
cha kukunjwa.[j] **5** Kisha Yere-
mia akamwamuru Baruku, aki-
sema: "Nimefungiwa. Siwezi
kuingia katika nyumba ya Ye-
hova.[k] **6** Na wewe mwenye-
we utaingia na kusoma kwa sau-
ti katika kitabu cha kuku-
njwa ambacho umeandika ku-
pitia kinywa changu maneno
ya Yehova[l] masikioni mwa watu
katika nyumba ya Yehova kati-
ka siku ya kufunga;[m] na pia ma-
sikioni mwa Yuda wote wanao-
ingia kutoka katika majiji yao
unapaswa kuyasoma kwa sau-
ti.[n] **7** Labda ombi lao la ku-
taka kibali litaanguka mbele
za Yehova[o] nao watarudi, kila
mtu kutoka katika njia yake
mbaya,[p] kwa maana hasira
na ghadhabu ni kuu ambazo
Yehova amesema juu ya watu
hawa."[q]

8 Na Baruku[r] mwana wa
Neria akafanya kulingana na
yote ambayo Yeremia nabii ali-
kuwa amemwamuru, kuso-
ma kwa sauti katika kile kita-
bu[a] maneno ya Yehova kwenye
nyumba ya Yehova.[b]

9 Sasa ikawa kwamba kati-
ka mwaka wa tano wa Yehoya-
kimu[c] mwana wa Yosia, mfa-
lme wa Yuda, katika mwezi wa
tisa,[d] watu wote katika Yeru-
salemu na watu wote waliokuwa
wakiingia Yerusalemu ku-
toka katika majiji ya Yuda wa-
litangaza kufunga mbele za
Yehova.[e] **10** Na Baruku aka-
anza kusoma kwa sauti kati-
ka kile kitabu maneno ya Yere-
mia kwenye nyumba ya Yeho-
va, ndani ya chumba cha kulia
chakula[f] cha Gemaria[g] mwana
wa Shafani[h] mwandikaji,[i] kati-
ka ua wa juu, kwenye mwingi-
lio wa lango jipya la nyumba ya
Yehova,[j] masikioni mwa watu
wote.

11 Na Mikaya mwana wa
Gemaria mwana wa Shafa-
ni[k] akayasikia maneno yote
ya Yehova katika kile kita-
bu. **12** Ndipo akashuka kwe-
nye nyumba ya mfalme, kwe-
nda katika chumba cha kulia
chakula cha mwandishi, na, ta-
zama! hapo ndipo wakuu wote
walikuwa wameketi, Elishama[l]
mwandishi na Delaya[m] mwa-
na wa Shemaya na Elnathani[n]
mwana wa Akbori[o] na Gema-
ria[p] mwana wa Shafani[q] na Se-
dekia mwana wa Hanania na
wakuu wengine wote. **13** Na
Mikaya[r] akawaambia maneno
yote ambayo alikuwa amesikia
wakati Baruku aliposoma kwa
sauti katika kile kitabu masiki-
oni mwa watu.[s]

14 Ndipo wakuu wote waka-
mtuma Yehudi[t] mwana wa Ne-
thania mwana wa Shelemia

SURA 36
a Kum 31:24
Yer 45:1
Eze 2:9
b Yer 30:2
c Yer 4:16
Yer 32:30
d Yer 1:5
Yer 25:9
e Yer 1:2
Yer 25:3
f Yer 26:3
g Isa 55:7
Yer 18:8
Eze 33:11
Yon 3:8
h Zb 130:4
Mik 7:18
i Yer 32:12
j Yer 45:1
k Yer 32:2
l Yer 7:2
Yer 22:2
m Mdo 27:9
n Yer 36:13
o 2Nya 33:12
p Yer 25:5
Yon 3:8
Zek 1:4
q 2Nya 34:21
r Yer 32:12
Yer 36:4
Yer 45:2

Safu ya 2
a Ne 8:3
b Yer 7:2
c 2Fa 23:36
Yer 35:1
d Ne 1:1
e 2Nya 20:3
Ne 9:1
Est 4:16
f 1Nya 28:12
g Yer 36:25
h 2Fa 22:8
Yer 39:14
Eze 8:11
i Ezr 7:6
Zb 45:1
j Yer 26:10
k 2Nya 34:20
l Yer 36:20
m Yer 36:25
n Yer 26:22
Yer 36:25
o 2Fa 22:14
Yer 26:22
p Yer 36:10
q 2Fa 22:8
Yer 26:24
Yer 39:14
r Yer 36:11
s Yer 36:21
t Yer 36:21

mwana wa Kushi kwa Baruku,[a] na kusema: "Kile kitabu cha kukunjwa ambacho ulisoma kwa sauti masikioni mwa watu—kichukue mkononi mwako uje." Basi Baruku mwana wa Neria akakichukua kile kitabu mkononi mwake, akaingia kwao.[b] **15** Kisha wakamwambia: "Tafadhali keti, ukisome kwa sauti masikioni mwetu." Kwa hiyo Baruku[c] akasoma kwa sauti masikioni mwao.

16 Sasa ikawa kwamba mara tu walipoyasikia yale maneno yote, wakaangaliana kwa hofu; nao wakamwambia Baruku: "Bila shaka tutamwambia mfalme maneno haya yote."[d] **17** Nao wakamuuliza Baruku, wakisema: "Tafadhali tuambie, Uliandikaje maneno haya yote kutoka kinywani mwake?"[e] **18** Ndipo Baruku akawaambia: "Aliendelea kunitangazia maneno haya yote kutoka kinywani mwake, nami nilikuwa nikiandika kwa wino katika kitabu."[f] **19** Mwishowe wakuu wakamwambia Baruku: "Nenda, jifiche, wewe pamoja na Yeremia, ili kwamba mtu yeyote asijue mahali mlipo."[g]

20 Kisha wakaingia kwa mfalme, kwenye ua,[h] nao wakakiweka kile kitabu cha kukunjwa katika chumba cha kulia chakula[i] cha Elishama[j] mwandishi; nao wakaanza kusema maneno yale yote masikioni mwa mfalme.

21 Kwa hiyo mfalme akamtuma Yehudi[k] kukichukua kile kitabu cha kukunjwa. Basi akakichukua kutoka katika chumba cha kulia chakula cha Elishama[a] mwandishi.[b] Na Yehudi akaanza kukisoma kwa sauti masikioni mwa mfalme na masikioni mwa wakuu wote waliokuwa wamesimama kando ya mfalme. **22** Na mfalme alikuwa ameketi katika nyumba ya majira ya baridi kali,[c] katika mwezi wa tisa,[d] na jiko la makaa[e] lilikuwa linawaka mbele yake. **23** Kisha ikawa kwamba mara tu Yehudi alipokuwa amesoma safu za kurasa tatu au nne, akakipasua kwa kisu cha mwandishi, na pia akakitupa katika moto uliokuwa katika lile jiko mpaka kitabu chote kilipoishia ndani ya ule moto uliokuwa katika jiko.[f] **24** Nao hawakuingiwa na hofu yoyote;[g] na mfalme wala watumishi wake wote, waliokuwa wakisikiliza maneno hayo yote, hawakurarua mavazi yao.[h] **25** Na hata Elnathani[i] na Delaya[j] na Gemaria[k] wakamsihi mfalme asiteketeze kile kitabu cha kukunjwa, lakini hakuwasikiliza.[l] **26** Na zaidi ya hayo, mfalme akawaamuru Yerahmeeli mwana wa mfalme na Seraya mwana wa Azrieli na Shelemia mwana wa Abdeeli waende kumleta Baruku mwandishi na Yeremia nabii.[m] Lakini Yehova akaendelea kuwaficha.[n]

27 Na neno la Yehova likamjia Yeremia tena baada ya mfalme kukiteketeza kile kitabu cha kukunjwa pamoja na yale maneno ambayo Baruku[o] alikuwa ameandika kutoka katika kinywa cha Yeremia,[p] na kusema: **28** "Chukua tena kitabu cha kukunjwa, kingine, nawe uandike juu yake yale maneno yote ya kwanza ya-

SURA 36

a Yer 36:26
b Yer 36:2
c Yer 45:1
d Amo 7:10
e Yer 36:4
f 3Yo 13
g Yer 36:26
h Yer 36:10
i 1Nya 28:12
j Yer 36:12
k Yer 36:14

Safu ya 2

a Yer 36:12
b 2Nya 34:18
c Amo 3:15
d Ezr 10:9
e Isa 47:14
f Zb 50:17
Isa 28:14
g Zb 36:1
h 2Fa 19:1
Isa 36:22
Mt 26:65
i 2Fa 24:8
Yer 26:22
j Yer 36:12
k Yer 36:10
l Met 21:29
m Yer 1:5
Mt 27:9
n 1Fa 17:3
Yer 1:19
2Pe 2:9
o Yer 32:12
Yer 45:1
p Yer 36:2

liyokuwa juu ya kile kitabu
cha kwanza, ambacho Yehoya-
kimu mfalme wa Yuda alite-
keteza.[a] **29** Nawe unapaswa
kusema hivi juu ya Yehoyaki-
mu mfalme wa Yuda, 'Yehova
amesema hivi: "Wewe mwe-
nyewe umekiteketeza hiki ki-
tabu cha kukunjwa,[b] ukise-
ma, 'Kwa nini umeandika juu
yake,[c] ukisema: "Mfalme wa
Babiloni atakuja bila sha-
ka na hakika ataiharibu nchi
hii na kumkomesha mwanada-
mu na mnyama kutoka ndani
yake"?'[d] **30** Kwa hiyo Yeho-
va amesema hivi juu ya Yeho-
yakimu mfalme wa Yuda, 'Ha-
takuwa na mtu yeyote anaye-
keti juu ya kiti cha ufalme cha
Daudi,[e] na maiti yake itaku-
wa kitu kilichotupwa nje[f] kwe-
nye joto wakati wa mchana
na kwenye baridi kali wakati
wa usiku. **31** Nami nitamto-
za hesabu yeye[g] na uzao wake
na watumishi wake kosa lao,[h]
nami nitaleta juu yao na juu
ya wakaaji wa Yerusalemu na
juu ya watu wa Yuda ule msi-
ba wote ambao nimesema juu
yao,[i] nao hawakusikiliza.'"'"[j]

32 Na Yeremia akachukua
kitabu kingine cha kukunjwa,
akampa Baruku mwana wa Ne-
ria, mwandishi,[k] ambaye alia-
ndika juu yake kutoka kinywa-
ni[l] mwa Yeremia maneno yote
ya kile kitabu ambacho Yeho-
yakimu mfalme wa Yuda aliku-
wa ameteketeza motoni;[m] na
maneno mengine mengi kama
hayo yakaongezwa kwenye
hayo.

37 Na Mfalme Sedekia[n]
mwana wa Yosia[o] akaa-
nza kutawala mahali pa Ko-
nia[p] mwana wa Yehoyakimu,[q]
ambaye Nebukadreza mfalme
wa Babiloni alimfanya kuwa
mfalme katika nchi ya Yuda.[a]
2 Na yeye na watumishi wake
na watu wa nchi hawakuyasi-
kiliza maneno ya Yehova[b]
ambayo alisema kupitia Yere-
mia nabii.[c]

3 Mfalme Sedekia akamtu-
ma Yehukali[d] mwana wa Shele-
mia na Sefania[e] mwana wa Ma-
aseya[f] kuhani kwa Yeremia na-
bii, na kusema: "Tafadhali, sali
kwa ajili yetu kwa Yehova Mu-
ngu wetu."[g] **4** Na Yeremia
alikuwa akiingia ndani na ku-
toka nje katikati ya watu,[h] kwa
sababu hawakuwa wamemtia
kizuizini. **5** Na kulikuwa na
jeshi la Farao lililotoka Misri;[i]
na Wakaldayo waliokuwa waki-
zingira Yerusalemu wakasi-
kia habari kuwahusu. Basi wa-
kaondoka mbele ya Yerusale-
mu.[j] **6** Kisha neno la Yehova
likamjia Yeremia nabii, na ku-
sema: **7** "Yehova Mungu wa
Israeli amesema hivi, 'Mwa-
mbieni hivi mfalme wa Yuda,
yeye aliyewatuma kwangu ku-
niuliza habari:[k] "Tazama! Je-
shi la Farao ambalo linawajia
ninyi kwa kusudi la kuwapa
msaada litarudi nchini kwao,
Misri.[l] **8** Na hakika Wakalda-
yo watarudi tena na kupiga
vita juu ya jiji hili na kuliteka
na kuliteketeza kwa moto."[m]
9 Yehova amesema hivi: "Msi-
zidanganye nafsi zenu,[n] mkise-
ma, 'Bila shaka Wakaldayo wa-
taenda zao waondoke juu
yetu,' kwa sababu hawataa-
nda zao. **10** Kwa maana iki-
wa mngelipiga na kuliua je-
shi lote la Wakaldayo wanao-
pigana nanyi[o] na kati yao wa-
baki watu waliochomwa,[p] kila

SURA 36

a Yer 36:23
b Yer 36:23
c Isa 30:10
Amo 5:10
d Yer 21:4
Yer 32:28
Yer 34:21
e 2Fa 24:8
2Fa 24:15
2Nya 36:10
Yer 22:30
f Yer 22:19
g Yer 21:14
h Isa 3:11
i Kum 28:15
Met 29:1
Yer 19:15
Yer 35:17
j 2Nya 36:16
k Yer 36:2
l Yer 36:4
Ro 16:22
m Yer 36:23

SURA 37

n 2Fa 24:18
1Nya 3:15
o 2Fa 23:28
p 2Fa 24:12
1Nya 3:16
2Nya 36:9
Yer 22:24
q 2Fa 24:6
Da 1:1

Safu ya 2

a 2Fa 24:17
2Nya 36:10
b 2Fa 24:19
c Ho 12:10
d Yer 38:1
e 2Fa 25:18
Yer 21:1
Yer 52:24
f Yer 29:25
g Yer 21:2
Yer 42:2
h Yer 32:2
Yer 37:15
i Eze 17:15
j Yer 34:21
k Yer 21:2
l Isa 30:3
Isa 31:3
Yer 17:5
Omb 4:17
Eze 17:17
m Yer 32:29
Yer 34:22
Yer 38:23
Yer 39:8
n Oba 3
o Yer 21:4
p Yer 51:4

mmoja wao angesimama katika hema lake na kuliteketeza jiji hili kwa moto.”’”

11 Na ikawa kwamba wakati jeshi la Wakaldayo lilipokuwa limejiondoa juu ya Yerusalemu[a] kwa sababu ya jeshi la Farao,[b] **12** Yeremia akaanza kuondoka Yerusalemu ili kwenda katika nchi ya Benyamini[c] na kupata fungu lake kutoka huko katikati ya watu. **13** Basi ikawa kwamba alipokuwa katika Lango la Benyamini,[d] yule ofisa aliyekuwa mwangalizi ambaye jina lake lilikuwa Iriya mwana wa Shelemia mwana wa Hanania, alikuwa hapo. Mara moja akamshika Yeremia nabii, akisema: “Unakimbia kwenda kwa Wakaldayo!” **14** Lakini Yeremia akasema: “Ni uwongo![e] Mimi sikimbii kwenda kwa Wakaldayo.” Lakini yeye hakumsikiliza. Basi Iriya akaendelea kumshika Yeremia na kumleta kwa wakuu. **15** Na wakuu[f] wakaanza kumkasirikia Yeremia,[g] nao wakampiga[h] na kumtia katika nyumba ya pingu,[i] katika nyumba ya Yehonathani[j] mwandishi, kwa maana walikuwa wameifanya hiyo kuwa kizuizi.[k] **16** Yeremia alipokuja ndani ya nyumba ya tangi la maji[l] na ndani ya vyumba vyenye ngome, ndipo Yeremia akaendelea kukaa humo siku nyingi.

17 Na Mfalme Sedekia akatuma watu kumchukua, na mfalme akaanza kumuuliza maswali katika nyumba yake mahali pa maficho.[m] Naye akaendelea kusema: “Je, liko neno lolote kutoka kwa Yehova?” Yeremia akasema: “Liko!” Naye akaendelea kusema: “Utatiwa mkononi mwa mfalme wa Babiloni!”[a]

18 Kisha Yeremia akamwambia Mfalme Sedekia: “Ni kwa njia gani nimetenda dhambi juu yako na juu ya watumishi wako na juu ya kikundi hiki cha watu,[b] hivi kwamba mmenitia kizuizini? **19** Wako wapi, sasa, manabii wenu waliowatolea unabii, wakisema, ‘Mfalme wa Babiloni hatakuja juu yenu na juu ya nchi hii’?[c] **20** Na sasa, sikiliza, tafadhali, Ee bwana wangu mfalme. Tafadhali, ombi langu la kibali[d] na lifike mbele yako, nawe usinirudishe katika nyumba ya Yehonathani[e] mwandishi, nisije nikafa humo.”[f] **21** Ndipo Mfalme Sedekia akatoa amri, kisha wakamtia Yeremia kifungoni katika Ua wa Walinzi;[g] wakampa mkate wa mviringo kila siku kutoka kwenye barabara ya waokaji,[h] mpaka mkate wote ulipokwisha jijini.[i] Na Yeremia akaendelea kukaa katika Ua wa Walinzi.[j]

38 Na Shefatia mwana wa Matani na Gedalia mwana wa Pashuri na Yukali[k] mwana wa Shelemia na Pashuri mwana wa Malkiya[l] wakayasikia maneno ambayo Yeremia alikuwa akiwaambia watu wote,[m] akisema: **2** “Yehova amesema hivi, ‘Yule anayeendelea kukaa ndani ya jiji hili ndiye atakayekufa kwa upanga,[n] kwa njaa[o] na kwa tauni.[p] Lakini yule atakayetoka nje kuwaendea Wakaldayo ndiye atakayeendelea kuishi na ndiye ambaye hakika nafsi yake itakuwa kama nyara kwake na ikiwa hai.’[q] **3** Yehova amese-

SURA 37
a Yer 34:21
Yer 37:5
b Eze 17:15
c Yos 18:28
Yer 1:1
d Yer 38:7
e Zb 27:12
Zb 35:11
f Yer 38:4
g Yer 26:11
h Lu 20:10
2Ko 11:23
Ebr 11:36
i 2Nya 16:10
Yer 20:2
Mdo 5:18
Mdo 12:6
j Yer 38:26
k Yer 37:4
l Yer 38:6
m Yer 38:14

Safu ya 2
a Yer 21:7
Yer 24:8
Yer 34:21
Eze 12:13
b 1Sa 26:18
c Yer 14:13
Yer 23:17
Yer 27:14
Yer 28:2
Omb 2:14
d Yer 36:7
e Yer 37:15
f Yer 26:15
Yer 38:9
g Ne 3:25
Yer 32:2
Yer 33:1
Yer 38:13
Yer 38:28
h 1Fa 17:6
Zb 37:19
i Kum 28:53
2Fa 25:3
Yer 38:9
j Yer 38:13

SURA 38
k Yer 37:3
l Yer 21:1
m Yer 21:8
n Yer 21:9
o Yer 27:13
p Yer 29:18
Eze 6:11
Eze 7:15
q Yer 21:9
Yer 45:5

ma hivi, 'Bila shaka jiji hili litatiwa mkononi mwa jeshi la mfalme wa Babiloni, naye hakika ataliteka.'"[a]

4 Na wakuu wakaanza kumwambia mfalme: "Tafadhali, acha mtu huyu auawe,[b] kwa maana hivyo ndivyo anavyoidhoofisha mikono ya watu wa vita ambao wamebaki ndani ya jiji hili na mikono ya watu wote, kwa kuwaambia maneno haya.[c] Kwa maana mtu huyu hatafuti amani ya watu hawa bali msiba." **5** Kwa hiyo Mfalme Sedekia akasema: "Tazama! Yuko mikononi mwenu. Kwa maana hakuna jambo lolote ambalo mfalme anaweza kuwazuia ninyi."[d]

6 Nao wakamchukua Yeremia na kumtupa ndani ya tangi la maji la Malkiya[e] mwana wa mfalme, lililokuwa katika Ua wa Walinzi.[f] Hivyo wakamshusha Yeremia ndani kwa kamba. Basi hapakuwa na maji ndani ya lile tangi, bali matope; na Yeremia akaanza kuzama katika yale matope.[g]

7 Na Ebed-meleki Mwethiopia,[h] mtu aliyekuwa towashi na aliyekuwa katika nyumba ya mfalme, akasikia kwamba walikuwa wamemtia Yeremia ndani ya tangi; na mfalme alikuwa ameketi katika Lango la Benyamini.[i] **8** Basi Ebed-meleki akatoka katika nyumba ya mfalme na kumwambia mfalme, akisema: **9** "Ee bwana wangu mfalme, watu hawa wametenda mabaya kwa yote ambayo wamemtendea Yeremia nabii, ambaye wamemtupa ndani ya tangi la maji, hivi kwamba atakufa[j] hapo alipo kwa sababu ya njaa.[k] Kwa maana hakuna mkate tena jijini."

10 Ndipo mfalme akamwamuru Ebed-meleki Mwethiopia, akisema: "Chukua watu 30 chini ya usimamizi wako kutoka mahali hapa, nawe umwondoe Yeremia nabii katika lile tangi kabla hajafa."[a] **11** Kwa hiyo Ebed-meleki akawachukua wale watu chini ya usimamizi wake, akaingia katika nyumba ya mfalme mpaka chini ya hazina[b] na kuchukua kutoka hapo vitambaa vizee-vizee na vipande vizee-vizee vya nguo na kuvishusha kwa Yeremia ndani ya lile tangi[c] kwa kamba. **12** Ndipo Ebed-meleki Mwethiopia akamwambia Yeremia: "Tafadhali, tia hivi vitambaa vizee-vizee na vipande vizee-vizee vya nguo katika makwapa yako chini ya kamba." Basi Yeremia akafanya hivyo.[d] **13** Mwishowe wakamvuta Yeremia nje kwa zile kamba na kumtoa ndani ya lile tangi. Na Yeremia akaendelea kukaa katika Ua wa Walinzi.[e]

14 Na Mfalme Sedekia akatuma watu na kumchukua Yeremia nabii[f] kwenye mlango wa tatu,[g] ulio katika nyumba ya Yehova,[h] kisha mfalme akamwambia Yeremia: "Ninakuuliza jambo fulani. Usinifiche jambo lolote."[i] **15** Ndipo Yeremia akamwambia Sedekia: "Ikiwa nitakuambia, je, hutaniua bila shaka? Na ikiwa nitakushauri, wewe hutanisikiliza."[j] **16** Kwa hiyo Mfalme Sedekia akamwapia Yeremia mahali pa maficho, akisema: "Kama anavyoishi Yehova, ambaye ametufanyia sisi nafsi[k] hii, mimi sitakuua,

SURA 38

a 2Fa 25:1
2Nya 36:17
Yer 21:10
Yer 32:3
Yer 52:4

b Yer 26:11

c Amo 7:10

d Yoh 19:16

e Yer 38:13

f Yer 33:1
Yer 37:21
Yer 38:28

g Mwa 37:24
Zb 109:5
Omb 3:53

h Yer 39:16
Mdo 8:27

i Yer 37:13

j Met 24:11

k Yer 52:6

Safu ya 2

a Zb 75:10
Zb 82:4
Met 21:1

b 2Fa 20:13

c Met 3:27
Yer 38:6

d Mt 10:41

e Yer 37:21

f Yer 21:1

g 2Fa 16:18

h Yer 20:2

i 1Sa 3:17
1Fa 22:16

j Lu 22:67

k Mwa 2:7
Kum 4:32
Isa 57:16
Yer 27:5

wala sitakutia mkononi mwa watu hawa wanaoitafuta nafsi yako.”[a]

17 Basi Yeremia akamwambia Sedekia: “Yehova, Mungu wa majeshi,[b] Mungu wa Israeli,[c] amesema hivi, ‘Bila shaka ukitoka nje kwenda kwa wakuu wa mfalme wa Babiloni,[d] hakika nafsi yako itaendelea kuishi na jiji hili halitateketezwa kwa moto, na wewe mwenyewe na nyumba yako hakika mtaendelea kuishi.[e] **18** Lakini ikiwa hutaenda nje kwa wakuu wa mfalme wa Babiloni, jiji hili pia lazima litatiwa mkononi mwa Wakaldayo, nao kwa kweli wataliteketeza kwa moto,[f] nawe hutaponyoka mkononi mwao.’”[g]

19 Kisha Mfalme Sedekia akamwambia Yeremia: “Ninawaogopa Wayahudi ambao wamekimbia kwenda kwa Wakaldayo,[h] wasije wakanitia katika mikono yao nao wakanitendea vibaya.”[i] **20** Lakini Yeremia akasema: “Hawatakutia mkononi mwao. Tafadhali, itii sauti ya Yehova kwa habari ya mambo ninayokuambia, na itakuwa vema kwako,[j] na nafsi yako itaendelea kuishi. **21** Lakini ikiwa unakataa kwenda nje,[k] hili ndilo jambo ambalo Yehova amenionyesha: **22** Na, tazama! wanawake wote ambao wameachwa katika nyumba ya mfalme wa Yuda[l] wanatolewa nje kwa wakuu wa mfalme wa Babiloni,[m] nao wanasema,

‘Watu wanaoishi kwa amani pamoja nawe wamekushawishi[n] na kukushinda.[o]
Wamefanya mguu wako uzame chini katika matope; wamerudi nyuma kwenda upande ule mwingine.’[a]

23 Nao wanawatoa nje wake zako wote na wana wako wote na kuwapeleka kwa Wakaldayo, nawe mwenyewe hutaponyoka mkononi mwao,[b] lakini utakamatwa kwa mkono wa mfalme wa Babiloni, na kwa sababu yako jiji hili litateketezwa kwa moto.”[c]

24 Na Sedekia akamwambia Yeremia: “Mtu yeyote asijue mambo haya, ili usife. **25** Na ikiwa wakuu[d] watasikia kwamba nimesema nawe nao kwa kweli waje kwako na kukuambia, ‘Tafadhali, tuambie, Ulimwambia nini mfalme? Usitufiche jambo lolote, nasi hatutakuua. Na mfalme alikuambia habari gani?’ **26** wewe pia utawaambia, ‘Nilikuwa nikitoa mbele ya mfalme ombi langu la kutaka kibali, kwamba asinirudishe katika nyumba ya Yehonathani[e] ili nisife humo.’”

27 Baadaye wakuu wote wakamjia Yeremia na kuanza kumuuliza maswali. Yeye naye akawaambia kulingana na maneno hayo yote ambayo mfalme alikuwa ameamuru.[f] Kwa hiyo wakanyamaza mbele yake, kwa maana habari hiyo haikusikiwa. **28** Na Yeremia akaendelea kukaa katika Ua wa Walinzi[g] mpaka siku ambayo Yerusalemu lilitekwa.[h] Na hilo likatukia wakati tu ambapo Yerusalemu lilitekwa.[i]

39 Katika mwaka wa tisa wa Sedekia mfalme wa Yuda, katika mwezi wa kumi,[j] Nebukadreza mfalme wa Ba-

SURA 38
a Yer 15:21
Yer 26:24
b Zb 80:7
c 1Nya 17:24
Yer 31:23
d 2Fa 25:27
e Yer 21:9
Yer 27:12
f 2Fa 25:9
Yer 34:2
g 2Fa 25:6
Yer 39:5
Yer 52:8
h Met 29:25
i 1Sa 31:4
j 2Nya 20:20
Yer 7:23
Yer 26:13
k Met 1:24
l Yer 43:6
m Yer 39:3
n Zb 41:9
Met 16:29
o Omb 1:2

Safu ya 2
a Yer 46:5
Yer 46:21
b 2Fa 25:7
2Nya 36:20
Yer 39:6
Yer 52:8
c Yer 52:13
d Yer 36:12
Yer 38:4
e Yer 37:15
Yer 37:20
f Yos 2:5
Zb 39:1
g Yer 32:2
Yer 33:1
h Zb 23:4
Yer 15:20
Yer 37:21
Yer 39:14
i 2Fa 25:8
2Nya 36:17

SURA 39
j Eze 24:1

biloni na jeshi lake lote alikuja
Yerusalemu na kuanza kulizingira.[a]
2 Katika mwaka wa kumi
na moja wa Sedekia, katika mwezi wa nne, katika siku
ya tisa ya mwezi huo, jiji likapenywa.[b] **3** Na wakuu wote
wa mfalme wa Babiloni wakaingia na kuketi katika Lango la Kati,[c] yaani, Nergal-shareza, Samgar-nebo, Sarsekimu, Rabsarisi, Nergal-shareza yule Rabmagi na wakuu wengine wote wa mfalme wa Babiloni.
4 Sasa ikawa kwamba mara
tu Sedekia mfalme wa Yuda na watu wote wa vita walipowaona, wakaanza kukimbia[d] na kwenda nje ya jiji wakati wa usiku kupitia njia ya bustani ya mfalme,[e] kupitia lile lango lililo katikati ya zile kuta mbili; nao wakaendelea kutoka nje kupitia njia ya Araba.[f] **5** Na jeshi la Wakaldayo likawafuatilia,[g] nao wakamfikia Sedekia katika nchi tambarare ya jangwa la Yeriko.[h] Kisha wakamchukua na kumleta kwa Nebukadreza mfalme wa Babiloni kule Ribla[i] katika nchi ya Hamathi[j] ili atangaze hukumu juu yake.[k] **6** Na mfalme
wa Babiloni akawaua[l] wana wa Sedekia katika Ribla mbele ya macho yake,[m] na mfalme wa Babiloni akawaua watu wote wenye vyeo wa Yuda.[n]
7 Naye akayapofusha macho
ya Sedekia,[o] kisha akamfunga kwa pingu za shaba, ili ampeleke Babiloni.
8 Na Wakaldayo wakateketeza kwa moto nyumba ya mfalme na nyumba za watu,[p] nao wakazibomoa kuta za Yerusalemu.[a] **9** Na Nebuzaradani[b]
mkuu wa walinzi[c] akawapeleka uhamishoni kule Babiloni[d] wale watu wengine walioachwa ndani ya jiji, na wale waliokimbia ili kujiunga naye, na watu wengine walioachwa.
10 Na baadhi ya watu, watu
wa hali ya chini ambao hawakuwa na chochote hata kidogo, Nebuzaradani mkuu wa walinzi akawaacha wabaki katika nchi ya Yuda;[e] naye akawapa mashamba ya mizabibu na utumishi wa lazima katika siku hiyo.[f]
11 Zaidi ya hayo, Nebuka-
dreza mfalme wa Babiloni akatoa amri kumhusu Yeremia kupitia Nebuzaradani mkuu wa walinzi, akisema: **12** "Mchukue, nawe umwangalie sana,
wala usimtendee jambo lolote baya.[g] Lakini vile atakavyokuambia, wewe mtendee vivyo hivyo."[h]
13 Kwa hiyo Nebuzaradani[i]
mkuu wa walinzi na Nebushazbani yule Rabsarisi, na Nergal-shareza yule Rabmagi na wakuu wote wa mfalme wakawatuma watu; **14** naam, wa-
liwatuma watu na kumchukua Yeremia kutoka katika Ua wa Walinzi[j] na kumtia mkononi mwa Gedalia[k] mwana wa Ahikamu[l] mwana wa Shafani,[m] ili amlete katika nyumba yake, ili akae katikati ya watu.
15 Na neno la Yehova lika-
mjia Yeremia alipokuwa amefungiwa katika Ua wa Walinzi,[n] na kusema: **16** "Nenda,
umwambie Ebed-meleki[o] Mwethiopia, 'Yehova wa majeshi, Mungu wa Israeli, amesema hivi: "Tazama, ninayatimiza maneno yangu juu ya jiji hili

SURA 39
a 2Fa 25:2 Yer 52:4
b 2Fa 25:4 Yer 52:7 Eze 33:21
c Yer 1:15
d Kum 28:25
e 2Fa 25:4
f Kum 1:7
g Yer 32:4 Yer 38:18
h Yos 5:10 Yer 52:8
i 2Fa 23:33 2Fa 25:6 2Fa 25:21 Yer 52:26
j Yos 13:5 Amu 3:3 2Fa 17:24
k Yer 52:9
l 2Fa 25:7 Yer 52:10
m Kum 28:34 Isa 13:16
n Yer 21:7 Yer 34:19
o 2Fa 25:7 Yer 52:11 Eze 12:13
p 2Fa 25:9 2Nya 36:19 Isa 5:9 Yer 38:18

Safu ya 2
a 2Fa 25:10 Ne 1:3 Yer 52:14
b Yer 52:12
c 2Fa 25:20 Yer 40:1
d 2Fa 25:11
e Yer 52:16
f 2Fa 25:12
g Yer 40:4
h Met 16:7 Met 21:1
i 2Fa 25:20 Yer 40:1 Yer 52:12
j Yer 38:28
k 2Fa 25:22 Yer 40:5 Yer 41:2
l 2Nya 34:20 Yer 26:24
m 2Fa 22:8
n Yer 32:2 Yer 36:5 Yer 37:21
o Yer 38:7

kuwe msiba wala si mema,[a]
nayo hakika yatatimia mbele
yako katika siku ile.”’[b]
17 “‘Nami nitakukomboa
wewe katika siku ile,’[c] asema
Yehova, ‘nawe hutatiwa mko-
noni mwa watu ambao unawa-
ogopa.’[d]
18 “‘Kwa maana bila shaka
nitakuokoa, nawe hutaanguka
kwa upanga; na hakika nafsi
yako itakuwa kama nyara kwa-
ko,[e] kwa sababu umenitege-
mea mimi,’[f] asema Yehova.”

40 Neno lililomjia Yeremia
kutoka kwa Yehova baa-
da ya Nebuzaradani[g] mkuu wa
walinzi kumtoa katika Rama,[h]
alipomchukua huku akiwa
amefungwa kwa pingu za mko-
noni katikati ya wahamishwa
wote wa Yerusalemu na wa
Yuda, ambao walikuwa waki-
pelekwa uhamishoni kati-
ka Babiloni.[i] **2** Ndipo yule
mkuu wa walinzi akamchukua
Yeremia na kumwambia: “Ye-
hova Mungu wako alitangaza
msiba huu juu ya mahali hapa,[j]
3 ili Yehova autimize na ku-
fanya jinsi ambavyo amesema,
kwa sababu ninyi mumemte-
ndea Yehova dhambi wala ha-
mkuitii sauti yake. Na jambo
hili limewapata ninyi.[k] **4** Na
sasa, tazama! Leo nimekufu-
ngua pingu zilizokuwa miko-
noni mwako. Ikiwa ni vema
machoni pako uje pamoja nami
kule Babiloni, njoo, nami ni-
takuangalia sana.[l] Lakini iki-
wa ni vibaya machoni pako
kwenda pamoja nami kule Ba-
biloni, acha. Angalia! Nchi nzi-
ma iko mbele yako. Kokote
ambako ni kwema na sawa ma-
choni pako kwenda, nenda
huko.”[m]

SURA 39
a 2Nya 36:21; Da 9:12
b Zb 91:8
c Zb 41:1; Zb 50:15; Zb 91:14
d 2Sa 24:14
e Yer 21:9; Yer 45:5
f 1Nya 5:20; Zb 37:3; Zb 37:40; Zb 84:12; Yer 17:7

SURA 40
g 2Fa 25:20; Yer 39:9; Yer 52:12
h Yos 18:25; Amu 4:5
i Yer 39:14
j Kum 29:25; 1Fa 9:9
k Yer 50:7; Da 9:11; Ro 2:5
l Yer 39:12
m Mwa 20:15

Safu ya 2
a 2Fa 25:22; Yer 39:14; Yer 41:2
b 2Fa 22:12; 2Nya 34:20; Yer 26:24
c 2Fa 22:8
d Ezr 7:6; Met 16:7; Met 21:1; Yer 15:11
e Mdo 27:3
f Yer 39:14
g Amu 20:1; 1Fa 15:22
h 2Fa 25:23
i 2Fa 25:22; Yer 39:10; Yer 52:16
j 2Fa 25:25; Yer 41:1
k Yer 41:11; Yer 41:16; Yer 42:1
l 2Sa 23:28; 1Nya 2:54; 1Nya 11:30
m 2Fa 25:23; Yer 42:1
n Kum 3:14; Yos 12:5
o Yer 41:3
p 2Fa 25:22; Yer 39:14; Yer 41:2
q 2Fa 22:12; 2Nya 34:20; Yer 26:24
r 2Fa 22:8
s 1Sa 20:17; 2Fa 25:24
t Zb 37:3; Yer 27:11

5 Na alipokuwa bado haja-
amua kurudi, Nebuzaradani
akasema: “Rudi kwa Gedalia[a]
mwana wa Ahikamu[b] mwana
wa Shafani,[c] ambaye mfalme
wa Babiloni amemweka juu ya
majiji ya Yuda, nawe ukae pa-
moja naye katikati ya watu; au
popote ambapo ni sawa macho-
ni pako kwenda, nenda.”[d]
Ndipo mkuu wa walinzi aka-
mpa posho ya chakula na zawa-
di na kumwacha aende zake.[e]
6 Kwa hiyo Yeremia akaja kwa
Gedalia[f] mwana wa Ahikamu
kule Mispa[g] na kuanza kukaa
pamoja naye katikati ya watu
waliobaki katika nchi.
7 Baadaye wakuu wote wa
majeshi waliokuwa uwanjani,[h]
wao pamoja na watu wao, wa-
kasikia kwamba mfalme
wa Babiloni amemweka Geda-
lia mwana wa Ahikamu juu ya
nchi na kwamba alikuwa ame-
mweka juu ya wanawake na
watoto wadogo na baadhi ya
watu wa hali ya chini wa nchi,
ambao hawakuwa wamepele-
kwa uhamishoni katika Babilo-
ni.[i] **8** Basi wakamwendea
Gedalia kule Mispa, Ishmaeli[j]
mwana wa Nethania na Yoha-
nani[k] na Yonathani, wana wa
Karea, na Seraya mwana wa
Tanhumethi na wana wa Efai
Mnetofa[l] na Yezania[m] mwana
wa yule Mmaakathi,[n] wao pa-
moja na watu wao.[o] **9** Na Ge-
dalia[p] mwana wa Ahikamu[q]
mwana wa Shafani[r] akawaapa-
pia[s] wao pamoja na watu wao,
akisema: “Msiogope kuwatu-
mikia Wakaldayo. Endeleeni
kukaa katika nchi na kumtu-
mikia mfalme wa Babiloni, na
itakuwa vema kwenu.[t] **10** Na

kwa habari yangu, tazama, ninakaa katika Mispa,[a] ili kusimama mbele ya Wakaldayo watakaokuja kwetu. Nanyi kusanyeni divai[b] na matunda ya wakati wa kiangazi na mafuta na mviweke katika vyombo vyenu na mkae katika majiji yenu ambayo mmeyateka."

11 Na Wayahudi wote waliokuwa katika Moabu na katikati ya wana wa Amoni na katika Edomu na wale waliokuwa katika nchi nyingine zote,[c] wao pia wakasikia kwamba mfalme wa Babiloni amewapa Yuda mabaki na kwamba alikuwa ameweka juu yao Gedalia[d] mwana wa Ahikamu mwana wa Shafani. **12** Na Wayahudi wote wakaanza kurudi kutoka mahali pote ambapo walikuwa wametawanywa, nao wakaendelea kuja nchini Yuda kwa Gedalia kule Mispa.[e] Nao wakakusanya divai na matunda ya wakati wa kiangazi kwa wingi sana.

13 Naye Yohanani[f] mwana wa Karea[g] na wakuu wote wa majeshi waliokuwa uwanjani,[h] wakamjia Gedalia kule Mispa. **14** Nao wakamwambia: "Je, hujui kabisa kwamba Baalisi mfalme wa wana wa Amoni,[i] amemtuma Ishmaeli[j] mwana wa Nethania[k] ili akupige nafsi yako akuue?" Lakini Gedalia mwana wa Ahikamu hakuwaamini.[l]

15 Na Yohanani[m] mwana wa Karea mwenyewe akamwambia Gedalia, mahali pa maficho katika Mispa: "Nataka kwenda, sasa, nimpige na kumuua Ishmaeli mwana wa Nethania, kwa kuwa hakuna mtu atakayejua.[n] Kwa nini akupige nafsi akuue, na kwa nini watu wote wa Yuda wanaokusanyika kwako watawanywe na mabaki ya Yuda yaangamie?"[a] **16** Lakini Gedalia[b] mwana wa Ahikamu[c] akamwambia Yohanani mwana wa Karea: "Usifanye jambo hili, kwa maana unasema uwongo kumhusu Ishmaeli."[d]

41 Kwa hiyo ikawa kwamba katika mwezi wa saba, Ishmaeli[e] mwana wa Nethania mwana wa Elishama[f] wa uzao wa kifalme[g] na aliye wa wakuu wa mfalme na watu wengine kumi pamoja naye[h] wakamjia Gedalia mwana wa Ahikamu kule Mispa.[i] Nao hapo wakaanza kula mkate pamoja kule Mispa.[j] **2** Ndipo Ishmaeli mwana wa Nethania na wale watu kumi waliokuwa pamoja naye wakasimama, wakampiga kwa upanga Gedalia mwana wa Ahikamu mwana wa Shafani.[k] Kwa hiyo akamuua mtu ambaye mfalme wa Babiloni alikuwa amemweka juu ya nchi.[l] **3** Na Wayahudi wote waliokuwa pamoja naye, yaani, pamoja na Gedalia, kule Mispa, na Wakaldayo waliokuwa hapo, yaani, watu wa vita, Ishmaeli akawapiga na kuwaua.

4 Na ikawa kwamba katika siku ya pili baada ya kuuawa kwa Gedalia, wakati hakuna mtu yeyote aliyejua habari hiyo,[m] **5** wakaja watu kutoka Shekemu,[n] kutoka Shilo[o] na kutoka Samaria,[p] watu 80 huku ndevu zao zikiwa zimenyolewa[q] na mavazi yao yakiwa yameraruliwa nao wakiwa wamejitia mikato,[r] na

SURA 40
a Yer 40:6
b Kum 16:13; Yer 39:10
c Yer 24:9
d Yer 39:14
e Amu 20:1; 1Sa 7:5; 1Fa 15:22
f Yer 41:11; Yer 42:1; Yer 43:2
g Yer 40:8
h Yer 40:7
i Yer 41:10
j Yer 40:8; Yer 41:2
k 2Fa 25:23
l Met 22:3
m Yer 41:11; Yer 43:2
n 1Sa 26:8

Safu ya 2
a 2Sa 21:17
b 2Fa 25:22; Yer 39:14
c 2Fa 22:12; 2Nya 34:20; Yer 26:24
d Yer 41:2

SURA 41
e 2Fa 25:23; Yer 40:14
f 2Fa 25:25
g Eze 17:13
h 2Fa 25:25
i Yer 40:6
j Zb 41:9
k 2Fa 25:25
l Yer 40:7
m Yer 40:15
n Yos 24:32; 1Fa 12:1
o Yos 18:1; Yer 7:12
p 1Fa 16:24
q Law 19:27
r Kum 14:1

mkononi mwao walikuwa na
toleo la nafaka na ubani[a] ili
wavilete katika nyumba ya Ye-
hova. **6** Basi Ishmaeli mwa-
na wa Nethania akatoka Mi-
spa ili kuwapokea, akilia
huku akitembea.[b] Na ikawa
kwamba mara tu alipokuta-
na nao, akawaambia: "Njooni
kwa Gedalia mwana wa Ahika-
mu." **7** Lakini ikatukia kwa-
mba mara tu walipokuja kati-
kati ya jiji, Ishmaeli mwana wa
Nethania akawaua na kuwatu-
pa ndani ya tangi la maji, yeye
na wale watu waliokuwa pamo-
ja naye.[c]

8 Lakini palikuwa na watu
kumi kati yao ambao walimwa-
mbia Ishmaeli mara moja: "Usi-
tuue, kwa maana sisi tuna ha-
zina zilizofichwa shambani,
ngano na shayiri na mafuta
na asali."[d] Kwa hiyo akajiepu-
sha, naye hakuwaua katikati
ya ndugu zao. **9** Sasa lile tan-
gi la maji ambamo Ishmaeli[e]
aliitupa mizoga yote ya wale
watu ambao aliwaua lilikuwa
tangi kubwa, ambalo Mfalme
Asa alitengeneza kwa sababu
ya Baasha mfalme wa Israeli.[f]
Hilo ndilo Ishmaeli mwana wa
Nethania alilijaza wale walio-
uawa.

10 Kisha Ishmaeli akawa-
chukua mateka mabaki yote ya
watu waliokuwa kule Mispa,[g]
binti za mfalme[h] na watu wote
waliokuwa wamebaki Mispa,[i]
ambao Nebuzaradani mkuu wa
walinzi alikuwa ameweka chi-
ni ya ulinzi wa Gedalia mwana
wa Ahikamu.[j] Kwa hiyo Ishma-
eli mwana wa Nethania aka-
wachukua mateka akaenda ili
avuke kwenda kwa wana wa
Amoni.[k]

SURA 41

a Law 2:1
b 2Sa 3:16
c Met 1:16
Isa 59:7
d Ayu 2:4
Met 13:8
Mhu 7:12
e 2Fa 25:23
Yer 40:8
f 1Fa 15:22
2Nya 16:6
g Yer 40:12
h Yer 43:6
i Yer 43:5
j Yer 40:7
k Yer 40:14

Safu ya 2

a Yer 42:1
Yer 43:2
b Yer 40:13
c 2Sa 2:13
d Yer 40:6
e 1Fa 20:20
Ayu 21:30
f 2Fa 25:23
Yer 42:1
g Yer 41:2

11 Baadaye Yohanani[a] mwa-
na wa Karea na wakuu wote
wa majeshi[b] waliokuwa pamo-
ja naye wakasikia ubaya wote
ambao Ishmaeli mwana wa Ne-
thania alikuwa ametenda.
12 Basi wakawachukua watu
wote na kwenda kupiga vita juu
ya Ishmaeli mwana wa Netha-
nia, wakampata kando ya yale
maji mengi yaliyokuwa katika
Gibeoni.[c]

13 Kisha ikawa kwamba
mara tu watu wote waliooku-
wa pamoja na Ishmaeli wa-
lipomwona Yohanani mwa-
na wa Karea na wakuu wote
wa majeshi waliokuwa pamo-
ja naye, wakaanza kushangi-
lia. **14** Na watu wote ambao
Ishmaeli alikuwa amewachu-
kua mateka kutoka Mispa[d] wa-
kageuka, wakarudi na kumwe-
ndea Yohanani mwana wa Ka-
rea. **15** Naye Ishmaeli mwa-
na wa Nethania akakimbia[e]
pamoja na watu wanane kuto-
ka mbele ya Yohanani, ili aende
kwa wana wa Amoni.

16 Sasa Yohanani[f] mwana
wa Karea na wale wakuu wote
wa majeshi waliokuwa pamo-
ja naye wakachukua yale ma-
baki yote ya watu ambao wali-
kuwa wamewarudisha kuto-
ka kwa Ishmaeli mwana wa
Nethania, kutoka Mispa, baa-
da ya yeye kumpiga na ku-
muua Gedalia[g] mwana wa
Ahikamu, watu hodari, wanau-
me wa vita, na wake na wa-
toto wadogo na maofisa wa ma-
kao ya mfalme, ambao aliru-
disha kutoka Gibeoni. **17** Basi
wakaenda na kuanza kufanya
makao katika mahali pa ku-
kaa pa Kimhamu palipokuwa

kando ya Bethlehemu,[a] ili wazidi kwenda na kuingia Misri,[b] **18** kwa sababu ya Wakaldayo;[c] kwa maana walikuwa wameogopa kwa sababu yao,[d] kwa kuwa Ishmaeli mwana wa Nethania alikuwa amempiga na kumuua Gedalia mwana wa Ahikamu,[e] ambaye mfalme wa Babiloni alikuwa amemweka juu ya nchi.[f]

42 Kisha wakuu wote wa majeshi na Yohanani[g] mwana wa Karea na Yezania[h] mwana wa Hoshaya[i] na watu wote, kuanzia aliye mdogo zaidi mpaka aliye mkubwa zaidi, wakakaribia **2** na kumwambia Yeremia nabii: "Tafadhali, ombi letu la kutaka kibali na lifike mbele yako, nawe usali kwa ajili yetu kwa Yehova Mungu wako,[j] kwa ajili ya mabaki hawa wote, kwa maana tumeachwa mabaki, wachache kati ya wengi,[k] kama macho yako yanavyotuona. **3** Yehova Mungu wako na atuambie njia tunayopaswa kuitembea na jambo tunalopaswa kulifanya."[l]

4 Ndipo Yeremia nabii akawaambia: "Nimesikia. Tazama, ninasali kwa Yehova Mungu wenu kulingana na maneno yenu;[m] na hakika itakuwa kwamba kila neno ambalo Yehova atawajibu ninyi mimi nitawaambia.[n] Sitazuilia neno lolote kutoka kwenu."[o]

5 Nao wakamwambia Yeremia: "Yehova na awe shahidi wa kweli na mwaminifu juu yetu[p] ikiwa hatutafanya sawasawa kulingana na kila neno ambalo Yehova Mungu wako atakutuma kwetu.[q] **6** Kama ni jema au ni baya, sauti ya Yehova Mungu wetu ambaye tunakutuma kwake ndiyo tutakayoitii, ili iwe vema kwetu kwa sababu tunaitii sauti ya Yehova Mungu wetu."[a]

7 Sasa ikawa kwamba mwishoni mwa siku kumi neno la Yehova likamjia Yeremia.[b] **8** Kwa hiyo akamwita Yohanani mwana wa Karea na wakuu wote wa majeshi waliokuwa pamoja naye na watu wote, kuanzia aliye mdogo zaidi mpaka aliye mkubwa zaidi;[c] **9** naye akawaambia: "Yehova Mungu wa Israeli, ambaye mlinituma kwake ili kufanya ombi lenu la kutaka kibali lifike mbele zake,[d] amesema hivi, **10** 'Ikiwa bila shaka mtaendelea kukaa katika nchi hii,[e] mimi pia nitawajenga ninyi wala sitawabomoa, nami nitawapanda ninyi wala sitawang'oa;[f] kwa maana hakika nitaujuta ule msiba ambao nimewaletea ninyi.[g] **11** Msiwe na hofu kwa sababu ya mfalme wa Babiloni, ambaye mnamwogopa.'[h]

"'Msiwe na hofu kwa sababu yake,'[i] asema Yehova, 'kwa maana mimi niko pamoja nanyi, ili kuwaokoa na kuwakomboa kutoka mkononi mwake.[j] **12** Nami nitawapa ninyi rehema, na hakika yeye atakuwa na rehema juu yenu na kuwarudisha kwenye nchi yenu.[k]

13 "'Lakini ikiwa mtasema: "Hapana; hatutakaa katika nchi hii!" ili kutoitii sauti ya Yehova Mungu wenu,[l] **14** mkisema: "Hapana, bali tutaenda katika nchi ya Misri,[m] ambapo hatutaona vita wala hatutaisikia sauti ya baragumu wala

SURA 41
a Mwa 35:19; Amu 17:7; 1Nya 2:51
b 2Fa 25:26; Isa 30:2; Yer 42:14; Yer 43:7
c Yer 21:4; Yer 37:5
d Yer 42:11
e Yer 41:2
f Yer 40:5

SURA 42
g Yer 40:8; Yer 40:13; Yer 41:11
h 2Fa 25:23
i Yer 43:2
j 1Sa 7:8; 1Sa 12:19; Isa 37:4; Yak 5:16
k Law 26:22; Kum 28:62; Isa 1:9
l Ezr 8:21; Met 3:6
m 1Sa 12:23
n 1Fa 22:14
o 1Sa 3:18; Mdo 20:20
p Amu 11:10; 1Sa 12:5; Mik 1:2; Mal 3:5
q Kut 19:8; Kum 5:27

Safu ya 2
a Kum 5:33; Kum 6:3; Yer 7:23
b 2Pe 1:21
c Yer 41:16; Yer 42:1
d Yer 42:2
e Zb 37:3
f Yer 24:6; Yer 31:28; Yer 33:7
g Kum 32:36; Yer 18:8; Yer 26:19; Mik 7:18
h Yer 41:18
i 2Nya 32:7
j Zb 46:7; Zb 68:20; Isa 43:5; Ro 8:31
k Kut 34:6; Ne 9:31; Zb 106:45; Met 16:7; Da 9:9
l Yer 44:16
m Yer 43:7

kushinda njaa kwa kukosa
mkate; na hapo ndipo tuta-
kapokaa";[a] **15** kwa hiyo hata
sasa sikieni neno la Yehova,
enyi mabaki ya Yuda. Yehova
wa majeshi, Mungu wa Israe-
li, amesema hivi: "Hakika ninyi
mkikaza nyuso zenu kuingia
Misri nanyi kwa kweli mwi-
ngie ili kukaa huko mkiwa wa-
geni,[b] **16** itatukia pia kwa-
mba ule upanga ambao mna-
ogopa utawafikia huko kati-
ka nchi ya Misri,[c] na ile njaa
ambayo mnaiogopa itawafuati-
lia kwa ukaribu mpaka Misri;[d]
nanyi mtakufa huko.[e] **17** Na
itakuwa kwamba watu wote
ambao wamekaza nyuso zao
kuingia Misri ili kukaa huko
wakiwa wageni ndio watakao-
kufa kwa upanga, kwa njaa
na kwa tauni;[f] nao hawatakuwa
na mwenye kuokoka wala
mwenye kuponyoka, kwa saba-
bu ya ule msiba ambao ninale-
ta juu yao."'[g]

18 "Kwa maana Yehova wa
majeshi, Mungu wa Israeli,
amesema hivi, 'Kama hasira
yangu na ghadhabu yangu zili-
vyomwagwa juu ya wakaaji wa
Yerusalemu,[h] ndivyo ghadha-
bu yangu itakavyomwagwa juu
yenu kwa sababu ya ninyi ku-
ingia Misri, na hakika mta-
kuwa laana na kitu cha ku-
shangaza na tukano na shutu-
ma,[i] nanyi hamtapaona maha-
li hapa tena.'[j]

19 "Yehova amesema dhidi
yenu, enyi mabaki ya Yuda.
Msiingie Misri.[k] Mnapaswa
kujua hakika kwamba ni-
metoa ushahidi juu yenu leo,[l]
20 kwamba mmetenda kosa
juu ya nafsi zenu;[m] kwa maa-
na ninyi wenyewe mmenituma
kwa Yehova Mungu wenu, mki-
sema, 'Sali kwa ajili yetu
kwa Yehova Mungu wetu; nawe
utuambie kulingana na kila
jambo ambalo Yehova Mungu
wetu atasema, nasi hakika tu-
tafanya.'[a] **21** Nami ninawaam-
bia ninyi leo, lakini hakika
hamtaitii sauti ya Yehova Mu-
ngu wenu wala jambo lolote
ambalo amenituma nalo kwe-
nu.[b] **22** Na sasa jueni haki-
ka kwamba kwa upanga,[c] kwa
njaa na kwa tauni mtakufa ka-
tika mahali pale panapowape-
ndeza ninyi kuingia ili kukaa
mkiwa wageni."[d]

43 Basi ikawa kwamba
mara tu Yeremia alipo-
maliza kuwaambia watu wote
maneno yote ya Yehova Mu-
ngu wao ambayo Yehova Mu-
ngu wao alikuwa amemtuma
nayo kwao, maneno hayo yote,[e]
2 Azaria mwana wa Hoshaya[f]
na Yohanani[g] mwana wa Ka-
rea na watu wote wenye kimbe-
lembele[h] wakamwambia Yere-
mia: "Ni uwongo ambao wewe
unasema.[i] Yehova Mungu wetu
hakukutuma, kusema, 'Msii-
ngie Misri kukaa humo mki-
wa wageni.'[j] **3** Bali Baruku[k]
mwana wa Neria anakucho-
chea juu yetu ili kututia mko-
noni mwa Wakaldayo, ili watu-
e au watupeleke uhamishoni
Babiloni."[l]

4 Na Yohanani mwana wa
Karea na wakuu wote wa ma-
jeshi na watu wote hawakuitii
sauti ya Yehova,[m] ili waendelee
kukaa katika nchi ya Yuda.[n]
5 Basi Yohanani mwana wa
Karea na wakuu wote wa maje-
shi wakachukua mabaki wote
wa Yuda waliokuwa wameru-

SURA 42
a Hes 11:5
b Kum 17:16
Yer 44:12
c Kum 28:45
Met 13:21
Eze 11:8
d Yer 44:13
Yer 44:27
e Yer 44:12
f Yer 24:10
Yer 42:22
g Yer 44:14
Yer 44:28
h 2Fa 25:9
2Nya 34:25
2Nya 36:16
Yer 7:20
Yer 39:8
Yer 52:4
Omb 2:4
Nah 1:6
i Yer 18:16
Yer 24:9
Yer 29:18
j Yer 22:10
Yer 22:27
k Kum 17:16
Isa 30:3
Isa 31:1
l 2Nya 24:19
Ne 9:26
Mal 3:5
m Met 8:36

Safu ya 2
a Yer 42:2
b Yer 7:24
Zek 7:11
c Yer 43:11
sababu ya kiu.[a]
Watoto wameomba
mkate.[b] Hakuna
anayewapa mkate huo.[c]

ה [*He'*]

5 Wale waliokuwa wakila
vitu vyenye kupendeza
wameshikwa na
mshangao barabarani.[d]
Wale waliokuwa
wakilelewa katika nguo
nyekundu[e]
wamekumbatia marundo
ya majivu.[f]

ו [*Waw*]

6 Adhabu kwa kosa la binti
ya watu wangu pia
inakuwa kubwa kuliko
adhabu kwa kosa la
dhambi ya Sodoma,[g]
Lililoangamizwa kama
kwa dakika moja, na
ambalo hakuna mikono
iliyojitokeza kulisaidia.[h]

ז [*Za'yin*]

7 Wanadhiri[i] wake walikuwa
safi kuliko theluji;[j]
walikuwa weupe kuliko
maziwa.
Kwa kweli walikuwa
wekundu[k] kuliko
marijani; kung'arishwa
kwao kulikuwa kama
yakuti.[l]

ח [*Chehth*]

8 Sura yao imekuwa nyeusi
kuliko weusi wenyewe.
Hawakutambuliwa
barabarani.[m]
Ngozi yao imekauka juu ya
mifupa yao.[n] Imekauka
kama mti.

ט [*Tehth*]

9 Wale waliouawa kwa upanga[a] wamekuwa bora kuliko wale waliouawa kwa njaa,[b]
Kwa sababu hao hudhoofika, wakichomwa kwa sababu ya ukosefu wa mazao ya shambani.

י [*Yohdh*]

10 Mikono ya wanawake wenye huruma imetokosa watoto wao wenyewe.[c]
Wamekuwa kama mkate wa kufariji mtu wakati wa kuvunjika kwa binti ya watu wangu.[d]

כ [*Kaph*]

11 Yehova ametimiza ghadhabu yake.[e] Amemwaga hasira yake inayowaka.[f]
Naye anawasha moto katika Sayuni, unaoteketeza misingi yake.[g]

ל [*La´medh*]

12 Wafalme wa dunia na wakaaji wote wa nchi yenye kuzaa hawakuwa wameamini[h]
Kwamba mpinzani na adui wataingia katika malango ya Yerusalemu.[i]

מ [*Mem*]

13 Kwa sababu ya dhambi za manabii wake, makosa ya makuhani wake,[j]
Mlikuwa katikati yake wale wanaomwaga damu ya waadilifu.[k]

נ [*Nun*]

14 Wametanga-tanga kama vipofu[l] barabarani.[m]
Wamechafuliwa na damu,[a]
Hivi kwamba hakuna wanaoweza kugusa mavazi yao.[b]

ס [*Sa´mekh*]

15 "Ondokeni njiani! Najisi!"[c] Wamewapaazia sauti. "Ondokeni njiani! Ondokeni njiani! Msiguse!"[d]
Kwa maana wamekosa makao.[e] Pia wametanga-tanga.[f] Watu wamesema kati ya mataifa: "Hawatakaa tena kama wageni.[g]

פ [*Pe´*]

16 Uso wa Yehova umewatawanya.[h] Hatawatazama tena.[i]
Watu hawataonyesha kujali hata kwa walio makuhani.[j] Hakika hawatawakubali hata walio wanaume wazee."[k]

ע [*´A´yin*]

17 Tukiwa tungali bado tunaishi, macho yetu huendelea kudhoofika bure kwa kutazamia msaada wetu.[l]
Wakati wa kutazama kwetu tumetazamia taifa ambalo haliwezi kuleta wokovu.[m]

צ [*Tsa·dheh´*]

18 Wamewinda hatua zetu[n] hivi kwamba hakuna kutembea katika viwanja vyetu vya watu wote.
Mwisho wetu umekaribia. Siku zetu zimetimia, kwa maana mwisho wetu umekuja.[o]

SURA 4

a Yer 38:2
b Yer 29:17
c Law 26:29
Kum 28:55
Omb 2:20
Omb 4:3
d Kum 28:57
Isa 49:15
Omb 3:48
e Kum 28:20
2Nya 36:16
Yer 6:11
Yer 9:11
Eze 22:31
Da 9:12
Zek 1:6
f Law 26:28
Yer 7:20
g Kum 32:22
2Fa 25:9
h Kum 29:24
1Fa 9:8
i 2Fa 25:10
Yer 52:13
j Yer 5:31
Yer 6:13
Yer 14:14
Yer 23:11
Omb 2:14
Mik 3:11
Sef 3:4
k Yer 26:8
Mt 23:31
Lu 11:47
Mdo 7:52
l Isa 59:10
Sef 1:17
m Kum 28:28
Isa 56:10
Mt 15:14

Safu ya 2

a Hes 35:33
Isa 1:15
Yer 2:34
Eze 33:25
Ho 4:2
b Hes 19:16
c Law 13:45
d 2Ko 6:17
e Law 26:33
Omb 1:7
f Kum 28:65
g Kum 28:25
Kum 28:68
h Law 26:33
Kum 28:64
Yer 24:9
i Ayu 34:29
Zb 34:16
Isa 59:2
Yer 18:17
Ebr 8:9
j 2Fa 25:18
k Omb 5:12
Eze 9:6
l 2Fa 24:7
Isa 20:5
Omb 1:19
m Isa 30:3
Isa 31:3
Yer 37:7
Eze 29:6
n 2Fa 25:5
Yer 39:4
Omb 3:52
o Eze 7:2
Eze 12:23
Amo 8:2

ק [*Qohph*]

19 Wenye kutufuatilia
wamekuwa wepesi
kuliko tai wa mbinguni.[a]
Wametufuatilia vikali
juu ya milima.[b]
Wametuvizia nyikani.[c]

ר [*Rehsh*]

20 Pumzi ya mianzi ya
pua zetu,[d] mtiwa-mafuta
wa Yehova,[e] amenaswa
katika shimo lao
kubwa,[f]
Yule ambaye tumesema
habari zake: "Tutaishi
chini ya kivuli[g] chake
kati ya mataifa."[h]

ש [*Sin*]

21 Furahi na kushangilia,[i]
Ee binti Edomu,[j] wewe
unayekaa katika nchi ya
Usi.[k]
Kwako wewe pia kikombe
kitapita.[l] Utalewa na
kujionyesha ukiwa
uchi.[m]

ת [*Taw*]

22 Kosa lako, Ee binti
Sayuni, limefikia mwisho
wake.[n] Hatakupeleka
tena uhamishoni.[o]
Amegeuza fikira zake kwa
kosa lako, Ee binti
Edomu. Amefunua
dhambi zako.[p]

5 Ee Yehova, ukumbuke
yale yaliyotupata.[q]
Utazame, uone shutuma
zetu.[r]
2 Fungu la urithi wetu
limeenda kwa wageni,
nyumba zetu kwa watu
wa kutoka ugenini.[s]
3 Tumekuwa mayatima
wasio na baba.[t] Mama
zetu ni kama wajane.[u]
4 Tumetumia pesa ili
tunywe maji yetu
wenyewe.[a] Kuni zetu
wenyewe zinatujia kwa
bei.
5 Tumefuatiwa kwa ukaribu
kwenye shingo zetu.[b]
Tumechoka.
Hatukuachiwa pumziko
lolote.[c]
6 Tumewapa mkono[d] Misri;[e]
Ashuru,[f] ili tushibe
mkate.
7 Mababu zetu ndio
wamefanya dhambi.[g]
Hawako tena. Lakini
sisi, imekuwa lazima
tuchukue makosa yao.[h]
8 Watumishi wametawala
juu yetu.[i] Hakuna
anayetunyakua kutoka
mkononi mwao.[j]
9 Tunauleta mkate wetu
kwa kuhatarisha nafsi
zetu,[k] kwa sababu ya
upanga wa nyika.
10 Ngozi yetu imekuwa
moto kama tanuru, kwa
sababu ya maumivu ya
njaa.[l]
11 Wake wamenyenyekezwa
katika Sayuni,[m]
mabikira katika majiji ya
Yuda.
12 Wakuu wametundikwa
kwa mkono wao.[n] Hata
nyuso za wanaume
wazee
hazikuheshimiwa.[o]
13 Hata vijana wameinua
jiwe la kusagia la
mkononi,[p] na wavulana
wamejikwaa chini ya
kuni.[q]

SURA 4

a Kum 28:49; Isa 5:26; Yer 4:13; Ho 8:1; Hab 1:8
b 2Fa 25:5; Amo 2:14
c Omb 3:10
d Mwa 2:7
e Zb 89:20; Yer 37:1
f 2Fa 25:6; Yer 39:5; Yer 52:8; Eze 12:13
g Amu 9:15; Da 4:12
h 1Sa 9:16
i Met 2:14; 1Ko 13:6
j Zb 137:7; Oba 12
k Yer 25:20
l Yer 25:15; Yer 49:12; Oba 16
m Yer 49:10
n Law 26:43; Isa 40:2; Yer 50:20
o Law 26:44; Isa 52:1; Isa 60:18
p Zb 137:7; Isa 34:5; Eze 25:13; Eze 35:15; Amo 1:11; Oba 13

SURA 5

q Law 26:44; Yer 15:15; Omb 1:20
r Zb 44:13; Zb 79:4; Omb 2:15
s Kum 28:30; Zb 79:1; Zb 136:21; Isa 1:7; Yer 6:12; Sef 1:13
t Kut 22:24
u Yer 18:21

Safu ya 2

a Kum 28:48; Isa 3:1; Eze 4:11; Eze 4:16
b Kum 28:48; Yer 27:8; Yer 28:14
c Kum 28:65
d Eze 17:18
e Isa 30:2; Isa 31:1; Yer 2:18; Yer 2:36; Yer 44:12
f 2Nya 28:16; Ho 5:13; Ho 7:11; Ho 9:3; Ho 12:1
g Yer 16:12; Yer 31:29; Eze 18:2
h Kut 20:5; Yer 14:20; Zek 1:5
i Kum 28:43; Met 30:22; Isa 3:4

j Zek 11:6; k Yer 52:6; Eze 4:10; l 2Fa 25:3; Ayu 30:30; Omb 4:8; m Kum 28:30; Zek 14:2; n Yer 39:6; o Isa 47:6; Yer 6:11; Omb 4:16; p Amu 16:21; q Kut 1:11.

14 Wanaume wazee
wameacha kutoka
langoni,[a] vijana
wamekomesha muziki
wao wa vyombo.[b]
15 Furaha ya moyo wetu
imekoma. Mchezo wetu
wa dansi umebadilishwa
uwe maombolezo
matupu.[c]
16 Taji la kichwa chetu
limeanguka.[d] Ole wetu,
sasa, kwa sababu
tumefanya dhambi![e]
17 Kwa sababu hiyo
moyo wetu umekuwa
mgonjwa.[f] Kwa sababu
ya mambo haya macho
yetu yameingia giza,[g]
18 Kwa sababu ya mlima
wa Sayuni ambao
umefanywa ukiwa;[h]
mbweha wametembea
juu yake.[a]
19 Lakini wewe, Ee Yehova,
utaketi mpaka wakati
usio na kipimo.[b] Kiti
chako cha ufalme ni cha
kizazi baada ya kizazi.[c]
20 Kwa nini unatusahau
milele,[d] hivi kwamba
unatuacha kwa siku
nyingi?[e]
21 Uturudishe kwako,[f] Ee
Yehova, nasi tutarudi
bila kukawia. Utuletee
siku zilizo mpya kama
katika zamani za kale.[g]
22 Hata hivyo, hakika
umetukataa.[h]
Umetukasirikia sana.[i]

SURA 5
a Kum 16:18; Yos 20:4; Ru 4:11
b Yer 25:10
c Amo 8:10
d Ayu 19:9; Zb 7:5; Zb 89:39
e Met 14:34; Isa 3:9; Isa 59:12
f Isa 1:5; Yer 8:18; Omb 1:22
g Kum 28:65; Ayu 17:7; Zb 6:7; Isa 59:10; Omb 2:11
h Law 26:43; Yer 26:18

Safu ya 2
a Isa 32:14; Yer 9:11; Eze 13:4
b Zb 9:7; Zb 90:2; Zb 102:12
c Zb 102:27; Zb 145:13; Zb 146:10; Hab 1:12
d Zb 13:1; Yer 14:19
e Zb 79:5
f Kum 4:30; Zb 80:3; Zb 85:4; Yer 31:18; Yer 32:37;
g Yer 33:13; h Zb 44:9; i Kum 28:15; Zb 60:1; Yer 31:37.

EZEKIELI

1 Basi ikawa kwamba katika mwaka wa 30, mwezi wa 4, siku ya 5 ya mwezi huo, nilipokuwa kati ya watu waliohamishwa[a] kando ya mto Kebari,[b] mbingu zilifunguka[c] nami nikaanza kuona maono ya Mungu.[d] **2** Katika siku ya tano ya mwezi huo, yaani, katika mwaka wa tano wa uhamisho wa mfalme Yehoyakini,[e] **3** neno la Yehova likaja[f] moja kwa moja kwa Ezekieli[g] mwana wa Buzi kuhani katika nchi ya Wakaldayo[h] kando ya mto Kebari, nao mkono wa Yehova ukawa juu yake mahali pale.[i]

4 Nami nikaanza kuona, na, tazama! kulikuwa na upepo wenye tufani[a] ukija kutoka kaskazini, wingu kubwa sana[b] na moto wenye kutetemeka,[c] nalo lilikuwa linang'aa pande zote, na kutoka katikati yake kulikuwa na kitu kama mchanganyiko wa dhahabu na fedha, kutoka katikati ya moto.[d] **5** Na kutoka katikati yake kulikuwa na mfano wa viumbe hai wanne,[e] na hivi ndivyo walivyoonekana: walifanana na mtu wa udongo. **6** Na kila mmoja wao alikuwa na nyuso nne,[f] na kila mmoja wao alikuwa na mabawa manne.[g] **7** Na miguu yao ilikuwa miguu iliyonyooka, na wayo wa miguu yao

SURA 1
a 2Fa 24:14; Est 2:6
b Zb 137:1; Eze 3:15; Eze 10:15; Eze 43:3
c Mt 3:16; Mdo 7:55; Mdo 10:11; Ufu 19:11
d Mwa 15:1; Hes 12:6; Da 8:1
e 2Fa 24:12; 2Nya 36:10; Yer 24:1
f 2Pe 1:21
g Eze 24:24
h 2Fa 24:16; Yer 22:25
i 1Fa 18:46; 2Fa 3:15; Eze 3:14

Safu ya 2
a 1Fa 19:11
b Zb 97:2
c Kut 19:18; Kut 24:17
d Eze 8:2
e Eze 10:9; Ufu 4:6
f Eze 10:14; g Isa 6:2; Eze 10:21; Ufu 4:8.

ulikuwa kama wayo wa mguu
wa ndama;[a] nayo ilikuwa iking'aa kama mng'ao wa sha-
ba iliyong'arishwa.[b] **8** Na ku-
likuwako mikono ya mwanada-
mu chini ya mabawa yao pa-
nde zote nne,[c] na hao wanne
walikuwa na nyuso zao na ma-
bawa yao.[d] **9** Mabawa yao ya-
liungana pamoja. Hawakugeu-
ka walipokuwa wakienda; kila
mmoja wao alikuwa akienda
mbele moja kwa moja.[e]
10 Na mfano wa nyuso zao,
hao wanne walikuwa na uso
wa mwanadamu[f] na uso wa si-
mba[g] upande wa kuume,[h] na
hao wanne walikuwa na uso wa
ng'ombe-dume[i] upande wa ku-
shoto;[j] hao wanne pia waliku-
wa na uso wa tai.[k] **11** Hivyo
ndivyo nyuso zao zilivyoku-
wa. Nayo mabawa[l] yao ya liku-
wa yamenyooshwa nje kuele-
kea juu. Kila mmoja wao ali-
kuwa na mawili yakiwa ya-
meungana pamoja, na mawili
yaliifunika miili yao.[m]
12 Na kila mmoja wao aliku-
wa akienda mbele moja kwa
moja.[n] Popote ambapo roho ili-
taka kwenda, walienda.[o] Ha-
wakugeuka walipokuwa wakie-
nda.[p] **13** Na kuhusu mfano
wa hao viumbe hai, kuonekana
kwao kulikuwa kama makaa ya
moto yanayowaka.[q] Kitu kama
kuonekana kwa mienge[r] kili-
kuwa kikisonga mbele na nyu-
ma katikati ya hao viumbe hai,
nao moto ulikuwa mwanga-
vu, na umeme ulikuwa ukito-
ka kati ya moto.[s] **14** Na hao
viumbe hai walionekana kama
umeme katika kuondoka na ku-
rudi kwao.[t]
15 Nilipoendelea kuwaona
hao viumbe hai, tazama! ku-
likuwa na gurudumu moja du-
niani kando ya wale viu-
mbe hai,[a] kando ya zile nyu-
so nne za kila mmoja.[b] **16** Na
kuonekana kwa magurudumu[c]
hayo na muundo wake, kuli-
kuwa kama mng'ao wa krisoli-
to;[d] nayo yote manne yaliku-
wa mfano mmoja. Na kuone-
kana kwake na muundo wake
ni kama vile gurudumu lina-
vyokuwa katikati ya gurudu-
mu.[e] **17** Yalipoenda yaliweza
kwenda pande zote nne.[f] Ha-
yakugeuka upande mwingine
yalipoenda.[g] **18** Nayo mizi-
ngo yake, ilikuwa na kimo hivi
kwamba yaliogopesha; nayo
mizingo yake ilikuwa imejaa
macho kuyazunguka yote ma-
nne pande zote.[h] **19** Na wale
viumbe hai walipoenda, yale
magurudumu yalienda kando
yao, na wale viumbe hai wa-
lipoinuliwa kutoka duniani,
yale magurudumu yaliinuli-
wa.[i] **20** Popote ambapo roho
ilitaka kwenda, yalienda, roho
ikitaka kwenda huko; nayo
magurudumu yaliinuliwa juu
karibu nao kando yao, kwa
maana roho ya yule kiumbe
hai ilikuwa katika magurudu-
mu. **21** Walipoenda, hayo ya-
lienda; na waliposimama tuli,
nayo yalisimama tuli; na wali-
poinuliwa kutoka duniani, ma-
gurudumu yaliinuliwa juu ka-
ribu nao, kando yao, kwa maa-
na roho ya yule kiumbe hai ili-
kuwa katika magurudumu.[j]
22 Na juu ya vichwa vya
wale viumbe hai kulikuwa na
mfano wa anga[k] kama kume-
tameta kwa barafu yenye ku-
tia woga, lililotanda juu ya vi-
chwa vyao, upande wa juu.[l]
23 Na chini ya anga hilo ma-

SURA 1
a Law 11:3
b Da 10:6
Ufu 1:15
c Isa 6:6
Eze 10:8
d Eze 10:21
e Eze 10:11
f Ufu 4:7
g 2Sa 17:10
Met 28:1
h Eze 10:14
i Met 14:4
j Ufu 4:7
k Ayu 39:29
Met 30:19
Eze 10:14
l Zb 18:10
m Isa 6:2
n Eze 10:22
o Zb 103:20
Eze 1:20
Ebr 1:14
p Eze 1:17
q Zb 104:4
r Da 7:10
s Zb 97:3
t Zb 18:10
Mt 24:27

Safu ya 2
a Eze 10:9
Eze 10:13
Eze 11:22
b Ufu 4:7
c Eze 10:9
d Kut 39:13
Da 10:6
e Eze 10:10
Da 7:9
f Eze 10:11
g Eze 1:12
h Met 15:3
Eze 10:12
Zek 4:10
i Eze 10:16
j Eze 10:17
k Mwa 1:6
l Eze 10:1

bawa yao yalikuwa yamenyooka, moja kuelekea lingine. Kila mmoja alikuwa na mabawa mawili yakifunika upande huu na kila mmoja alikuwa na mawili yakifunika upande ule wa miili yao. **24** Nami nikasikia kishindo cha mabawa yao, kishindo kama kile cha maji mengi,[a] kama kishindo cha Yule Mweza-Yote, walipoenda, kishindo cha fujo,[b] kama kishindo cha kambi.[c] Waliposimama tuli, walikuwa wakiyashusha chini mabawa yao.

25 Na kukawa na sauti juu ya anga lililokuwa juu ya kichwa chao. (Waliposimama tuli, walikuwa wakiyashusha chini mabawa yao.) **26** Na juu ya anga lililokuwa juu ya kichwa chao kulikuwa na kitu kinachoonekana kama jiwe la yakuti,[d] mfano wa kiti cha ufalme.[e] Na juu ya kile kitu chenye mfano wa kiti cha ufalme kulikuwa na mfano wa mtu anayeonekana kama mtu wa udongo juu yake,[f] upande wa juu. **27** Nami nikaona kitu kama mng'ao wa mchanganyiko wa dhahabu na fedha,[g] kinachoonekana kama moto kuzunguka pande zote za ndani,[h] kuanzia kuonekana kwa kiuno chake kwenda juu; na kuanzia kuonekana kwa kiuno chake kwenda chini niliona kitu kinachoonekana kama moto, naye alikuwa na mwangaza kuzunguka pande zote. **28** Kulikuwa na kitu kinachoonekana kama upinde[i] ambao hutokea katika wingu kubwa katika siku ya mvua. Hivyo ndivyo ulivyokuwa mwangaza uliozunguka pande zote. Kulikuwa ni kuonekana kwa mfano wa utukufu wa Yehova.[a] Nilipouona, ndipo nikaanguka kifudifudi,[b] nami nikaanza kusikia sauti ya mtu anayesema.

2 Naye akaniambia: "Mwana wa binadamu,[c] simama kwa miguu yako ili nisieme nawe."[d] **2** Na roho ikaanza kuingia ndani yangu mara tu aliposema nami,[e] nayo mwishowe ikanifanya nisimame kwa miguu yangu ili nimsikie Yule anayesema nami.[f]

3 Naye akaendelea kuniambia: "Mwana wa binadamu, ninakutuma kwa wana wa Israeli,[g] kwa mataifa yenye kuasi ambayo yameniasi.[h] Hao wenyewe na mababu zao wamenitendea makosa mpaka siku hii ya leo.[i] **4** Na wana wenye uso wa dharau[j] na wenye moyo mgumu[k]—ninakutuma wewe kwao, nawe lazima utawaambia, 'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema.' **5** Nao, ikiwa watasikia[l] au watakataa[m]—kwa maana wao ni nyumba yenye kuasi[n]—hakika watajua pia kwamba nabii alikuwako katikati yao.[o]

6 "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, usiwaogope;[p] wala maneno yao usiyaogope, kwa sababu kuna wakaidi[q] na vitu vinavyokuwasha[r] nawe unakaa katikati ya nge.[s] Maneno yao usiyaogope,[t] nawe usiingiwe na hofu[u] kwa sababu ya nyuso zao, kwa maana wao ni nyumba yenye kuasi.[v] **7** Nawe utawaambia maneno yangu, bila kujali ikiwa watasikia au watakataa, kwa maana wao ni waasi.[w]

8 "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, sikia ninalokuambia. Usiwe mwasi kama ile nyumba

SURA 1

a Eze 43:2
Ufu 1:15
Ufu 14:2
b Ayu 37:2
Zb 29:3
Zb 68:33
c 2Fa 7:6
d Kut 24:10
Zb 96:6
Eze 10:1
e 1Fa 22:19
Zb 99:1
Isa 6:1
Ufu 4:2
f Da 7:9
g Eze 8:2
h Kum 4:24
Zb 104:2
i Mwa 9:13
Ufu 4:3

Safu ya 2

a Kut 24:16
Eze 8:4
b Eze 3:23
Eze 43:3
Da 8:17
Ufu 1:17

SURA 2

c Eze 8:5
Eze 37:3
d Da 10:11
e Eze 3:24
f Ufu 11:11
g 2Nya 36:15
Eze 33:7
Mt 10:16
h Zb 107:11
Isa 1:4
Isa 30:9
Yer 16:12
Omb 1:20
Da 9:9
i Kum 9:24
Ne 9:26
Zb 78:8
Yer 3:25
Eze 20:18
Mdo 7:51
j Mt 22:6
k Yos 11:20
Zb 95:8
Eze 3:7
Ebr 3:15
l Eze 33:15
m Eze 3:11
Eze 33:4
n Eze 12:2
o Eze 33:33
Yoh 15:22
p 2Fa 1:15
Met 29:25
Yer 1:17
Lu 12:4
q Kum 2:30
Mdo 7:51
r Isa 9:18
Mik 7:4
s Lu 10:19
t Eze 3:9
u Yer 1:8
v Isa 51:7
w Yer 1:17
Eze 3:27

yenye kuasi.[a] Fungua kinywa
chako ule ninachokupa."[b]
9 Nami nikaanza kuona, na,
tazama! kulikuwa na mkono uli-
onyooshwa kunielekea,[c] na, ta-
zama! kitabu cha kukunjwa ki-
likuwa ndani yake.[d] **10** Naye
akakikunjua mbele yangu ha-
tua kwa hatua, nacho kiliku-
wa kimeandikwa mbele na nyu-
ma;[e] nacho kilikuwa kimeandi-
kwa nyimbo za huzuni na mao-
mbolezo na vilio.[f]

3 Naye akaniambia: "Mwa-
na wa binadamu, kula una-
choona. Kula kitabu hiki cha
kukunjwa,[g] uende, ukaseme
na nyumba ya Israeli."
2 Kwa hiyo nikafungua ki-
nywa changu, naye hatua kwa
hatua akanilisha kile kitabu.[h]
3 Naye akaendelea kunia-
mbia: "Mwana wa binadamu,
unapaswa kulisha tumbo lako,
ili ujaze matumbo yako kwa ki-
tabu hiki ninachokupa wewe."
Nami nikaanza kukila, nacho
kikawa kitamu kama asali ki-
nywani mwangu.[i]
4 Naye akaendelea kunia-
mbia: "Mwana wa binada-
mu, nenda, uingie katikati ya
nyumba[j] ya Israeli, nawe lazi-
ma uwaambie maneno yangu.
5 Kwa maana hutumwi kwe-
nda kwa watu wa lugha isiyoele-
weka[k] wala walio wazito wa
ulimi[l]—kwa nyumba ya Israe-
li, **6** si kwa vikundi vya watu
wengi sana wa lugha isiyoele-
weka wala walio wazito wa ulimi,
ambao maneno yao huwezi
kuyasikia ukayafahamu.[m] Iki-
wa ningekutuma kwao, watu
hao wangekusikiliza wewe.[n]
7 Lakini nyumba ya Israe-
li, hawatataka kukusikiliza
wewe, kwa maana hawataki
kunisikiliza mimi;[a] kwa sababu
wote hao wa nyumba ya Israe-
li wana vichwa vigumu na mi-
oyo migumu.[b] **8** Tazama! Ni-
meufanya uso wako uwe mgu-
mu[c] kama nyuso zao na paji la
uso wako liwe gumu kama ma-
paji ya nyuso zao.[d] **9** Nimeli-
fanya paji la uso wako kuwa
kama almasi, gumu kuliko jiwe
gumu.[e] Usiwaogope,[f] wala usii-
ngiwe na hofu kwa sababu ya
nyuso zao,[g] kwa maana wao ni
nyumba yenye kuasi."[h]
10 Naye akaendelea kunia-
mbia: "Mwana wa binadamu,
maneno yangu yote nitakayo-
kuambia, yatie moyoni[i] mwa-
ko na usikie kwa masikio yako
mwenyewe. **11** Nawe uende,
uingie katikati ya watu wali-
ohamishwa,[j] katikati ya wana
wa watu wako, nawe utase-
ma nao na kuwaambia, 'Hivi
ndivyo Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema,' bila ku-
jali ikiwa watasikia au watakata-
taa."[k]
12 Nayo roho ikaniinua[l]
nami nikaanza kusikia nyu-
ma yangu kishindo cha mvumo
mkubwa:[m] "Na ubarikiwe utu-
kufu wa Yehova kutoka katika
mahali pake."[n] **13** Na kuli-
kuwa na kishindo cha mabawa
ya wale viumbe hai yaliyoku-
wa yakigusana karibu kari-
bu,[o] na kishindo cha magurudumu karibu nao kando yao,[p]
na kishindo cha mvumo mku-
bwa. **14** Nayo roho ikaniinua[q] na kunichukua, hivi kwa-
mba nikaenda kwa uchungu
katika ghadhabu ya roho ya-
ngu, na mkono wa Yehova juu
yangu ulikuwa wenye nguvu.[r]
15 Kwa hiyo nikaingia kati-

SURA 2

a Hes 20:24
Isa 50:5
b Yer 15:16
Ufu 10:9
c Yer 1:9
Eze 8:3
d Eze 3:1
Ufu 10:8
e Zek 5:3
Ufu 5:1
f Isa 3:11
Yer 7:29
Eze 19:1

SURA 3

g Eze 2:8
Ufu 10:9
h Ufu 10:10
i Zb 19:10
Zb 119:103
Yer 15:16
Ufu 10:9
j Mt 10:6
Mt 15:24
k Zb 81:5
Isa 33:19
l Kum 28:49
Isa 28:11
m Yer 5:15
n Yon 3:5
Mt 11:21
Mt 12:41
Mdo 13:46

Safu ya 2

a 1Sa 8:7
Yer 25:7
Lu 10:16
b Kut 34:9
Ne 9:16
Yer 3:3
Yer 5:3
Yer 7:26
Eze 2:4
c Yer 1:18
d Isa 50:7
Yer 15:20
Mik 3:8
e Isa 50:7
Zek 7:12
f Met 29:25
Isa 41:10
g Yer 1:18
Yer 17:18
h Eze 24:3
i Zb 119:11
Lu 8:15
j 2Fa 24:14
k Eze 2:5
Mdo 20:26
l 1Fa 18:12
2Fa 2:16
Eze 8:3
Mdo 8:39
m Mdo 2:2
n Eze 11:22
o Eze 1:24
p Eze 10:16
q Eze 8:3
r 1Fa 18:46
2Fa 3:15

kati ya watu waliohamishwa
huko Tel-abibu, waliokuwa wa-
kikaa[a] kando ya mto Kebari,[b]
nami nikaanza kukaa maha-
li walipokuwa wakikaa; nami
nikaendelea kukaa hapo kwa
siku saba, nikiwa nimepigwa
na bumbuazi katikati yao.[c]
16 Na ikawa kwamba mwi-
shoni mwa siku saba neno la
Yehova likanijia, na kusema:
17 "Mwana wa binadamu,
nimekufanya kuwa mlinzi ka-
tika nyumba ya Israeli,[d] nawe
utasikia maneno kutoka katika
kinywa changu nawe lazi-
ma utawapa maonyo kutoka
kwangu.[e] **18** Mimi ninapo-
mwambia mtu mwovu, 'Ha-
kika utakufa,'[f] na wewe usi-
mwonye na kusema ili kumwo-
nya mwovu aiache njia yake
ya uovu ili kumhifadhi hai,[g]
yeye akiwa ni mwovu, kati-
ka kosa lake atakufa,[h] lakini
damu yake nitaidai kutoka ka-
tika mkono wako mwenyewe.[i]
19 Lakini wewe, ikiwa ume-
mwonya mwovu[j] naye asigeuke
na kuuacha uovu wake na
njia yake ya uovu, yeye mwe-
nyewe atakufa kwa sababu ya
kosa lake;[k] lakini wewe, utaku-
wa umeiokoa nafsi yako mwe-
nyewe.[l] **20** Na mtu mwadilifu
anapogeuka na kuuacha ua-
dilifu[m] wake naye kwa kweli
atende kwa njia isiyo ya haki
nami nilazimike kuweka ki-
kwazo mbele yake,[n] yeye mwe-
nyewe atakufa kwa sababu hu-
kumwonya. Kwa sababu ya
dhambi yake atakufa,[o] na mate-
ndo yake ya uadilifu aliyoya-
tenda hayatakumbukwa,[p] laki-
ni damu yake nitaidai kutoka
katika mkono wako mwenye-
we.[a] **21** Na wewe, ikiwa ume-
mwonya mtu mwadilifu kwa-
mba mwadilifu huyo asitende
dhambi, naye mwenyewe ae-
puke kutenda dhambi,[b] hakika
ataendelea kuishi kwa sababu
alikuwa ameonywa,[c] na wewe
mwenyewe utakuwa umeiokoa
nafsi yako mwenyewe."[d]
22 Nao mkono wa Yehova
ukawa juu yangu huko, naye
akaniambia: "Ondoka, nenda
kwenye nchi tambarare ya bo-
ndeni,[e] na huko nitasema nawe."
23 Basi nikaondoka na kwe-
nda kwenye nchi tambarare ya
bondeni, na, tazama! utukufu
wa Yehova ulikuwa umesimama
huko,[f] kama utukufu niliouona
kando ya mto Kebari,[g] nami ni-
kaanguka kifudifudi.[h] **24** Ndi-
po roho ikaingia[i] ndani yangu
na kunifanya nisimame kwa
miguu yangu,[j] naye akaanza
kusema nami na kuniambia:
"Nenda, jifungie ndani ya
nyumba yako. **25** Na wewe,
Ee mwana wa binadamu, tazama!
hakika wataweka kamba
juu yako nao watatumia ka-
mba hizo kukufunga ili usi-
weze kwenda katikati yao.[k]
26 Nami nitaufanya ulimi
wako ushikamane na kaakaa
la kinywa chako,[l] nawe ha-
kika utakuwa bubu,[m] na kwao
wewe hutakuwa mtu mwenye
kutoa karipio,[n] kwa sababu
wao ni nyumba yenye kuasi.[o]
27 Nami ninaposema nawe,
nitakifungua kinywa chako,
nawe utawaambia,[p] 'Hivi ndi-
vyo Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova amesema.' Anayesi-
kia na asikie,[q] na anayekataa
na akataae, kwa sababu wao ni
nyumba yenye kuasi.[r]

SURA 3

a Yer 29:5
b Zb 137:1
Eze 1:3
Eze 43:3
c Yer 23:9
d Isa 21:8
Isa 62:6
Yer 6:17
Eze 33:7
e Isa 58:1
f 2Fa 1:4
g Mdo 2:40
1Ti 4:16
h Met 14:32
Eze 33:4
Ro 6:23
i Mwa 9:5
Eze 33:8
j 2Fa 17:13
k Ro 2:6
l Isa 49:4
Yer 45:5
Eze 33:9
Mdo 18:6
Mdo 20:26
m 2Nya 24:18
Eze 18:24
Eze 33:12
n Kum 13:3
1Pe 2:8
o Eze 18:26
Eze 33:18
p Eze 33:12

Safu ya 2

a Law 19:17
Eze 33:6
Ebr 13:17
b 1Sa 25:33
Mdo 20:31
c Met 17:10
Eze 33:15
Yak 5:20
d Mdo 18:6
e Eze 8:4
f Eze 1:28
g Eze 1:1
h Da 8:17
Ufu 4:10
i Eze 2:2
Eze 37:10
j Da 10:19
k Eze 4:8
Yoh 21:18
Mdo 20:23
l Zb 137:6
m Eze 24:27
Lu 1:22
n Amo 5:10
o Isa 1:2
Eze 2:6
p Eze 24:27
Eze 33:22
q Mt 11:15
Ufu 2:29
r Isa 30:9
Yer 5:23
Eze 12:2

4 "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, jichukulie tofali, nawe utaliweka mbele yako na kuchonga jiji juu yake, yaani, Yerusalemu.[a] **2** Nawe utalizingira[b] na kujenga ukuta wa kulizingira[c] na kuweka boma la kulizingira[d] na kuweka kambi kulizunguka na kuweka mitambo ya kubomolea kulizunguka pande zote.[e] **3** Na wewe, jichukulie kiokeo cha chuma, nawe utakiweka kuwa ukuta wa chuma kati yako na jiji hilo, nawe utaukaza uso wako juu yake, nalo litazingirwa, nawe utalizingira. Hiyo ni ishara kwa nyumba ya Israeli.[f]

4 "Na wewe, lalia upande wako wa kushoto, nawe utaweka kosa la nyumba ya Israeli juu yake.[g] Kwa hesabu ya siku utakazolalia upande huo utalichukua kosa lao. **5** Na mimi mwenyewe nitakupa wewe miaka ya kosa lao[h] kuwa hesabu ya siku 390,[i] nawe utalichukua kosa la nyumba ya Israeli. **6** Nawe lazima utazitimiza.

"Kisha utalalia upande wako wa kuume mara ya pili, nawe utalichukua kosa la nyumba ya Yuda kwa siku 40.[j] Nimekupa wewe siku moja kwa mwaka mmoja, siku moja kwa mwaka mmoja.[k] **7** Nawe utaukaza uso wako kuelekea kuzingirwa kwa Yerusalemu,[l] mkono wako ukiwa wazi, nawe utatoa unabii dhidi yake.

8 "Na, tazama! nitaweka kamba[m] juu yako ili usijigeuze kutoka upande wako mmoja mpaka upande wako mwingine, mpaka utakapokuwa umezitimiza siku za kuzingira kwako.

9 "Na wewe, jichukulie ngano[a] na shayiri na maharagwe mapana[b] na dengu[c] na mtama na kusemethi,[d] nawe utavitia katika chombo kimoja na kuvifanya kuwa mkate kwa ajili yako, kwa hesabu ya siku unazolalia upande wako; siku 390 utaula.[e] **10** Na chakula chako utakachokula kitakuwa kulingana na kipimo—shekeli 20 kwa siku.[f] Mara kwa mara utakila.

11 "Na maji utayanywa kulingana na kipimo, sehemu ya sita ya hini. Mara kwa mara utakunywa.

12 "Na kama keki ya mviringo ya shayiri[g] utaila; nayo, utaioka juu ya mashonde ya mavi[h] ya wanadamu mbele ya macho yao." **13** Na Yehova akaendelea kusema: "Hivyo ndivyo wana wa Israeli watakavyoula mkate wao ukiwa si safi[i] katikati ya mataifa ambako nitawatawanya."[j]

14 Nami nikasema: "Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Tazama! Nafsi yangu haijatiwa unajisi;[k] Sijala mnyama ambaye tayari amekufa wala mnyama aliyerarulia tangu ujana wangu,[l] mpaka sasa, na nyama chafu haijaingia kinywani mwangu."[m]

15 Basi akaniambia: "Tazama, nimekupa wewe mavi ya ng'ombe badala ya mashonde ya wanadamu, nawe utaufanya mkate wako juu yake." **16** Naye akaendelea kuniambia: "Mwana wa binadamu, tazama, ninavunja fimbo ambazo mikate ya mviringo huning'inizwa,[n] katika Yerusalemu, nao watalazimika kula mkate wao kulingana na kipimo na kwa

SURA 4

a Yer 32:31
b 2Fa 24:11
Yer 39:1
c 2Fa 25:1
Lu 19:43
d 2Sa 20:15
Yer 6:6
Yer 32:24
Eze 26:8
e Eze 21:22
f Eze 12:6
Eze 24:24
g 2Fa 17:21
h Hes 14:34
i 1Fa 12:19
j 2Fa 23:27
k Hes 14:34
l 2Nya 36:17
Yer 52:4
m Eze 3:25

Safu ya 2

a Kut 29:2
b 2Sa 17:28
c Mwa 25:34
d Kut 9:32
e Eze 4:5
f Law 26:26
g 2Fa 4:42
h Kum 23:13
i Law 19:19
j Ho 9:3
k Mdo 10:14
l Kut 22:31
Law 7:24
Law 11:40
m Law 7:18
Kum 14:3
Isa 65:4
Isa 66:17
n Law 26:26
Zb 105:16
Isa 3:1
Eze 5:16

hangaiko zito,[a] nao watakunywa maji kulingana na kipimo na kwa tisho,[b] **17** ili wapate kupungukiwa na mkate na maji nao watazamane kwa mshangao na kuoza kabisa katika kosa lao.[c]

5 "Na wewe, Ee Mwana wa binadamu, jichukulie upanga mkali. Utajichukulia ulio kama wembe wa kinyozi, nawe utaupitisha juu ya kichwa chako na juu ya ndevu zako,[d] nawe utajichukulia mizani ya kupimia na kuzigawanya nywele hizo katika mafungu. **2** Sehemu ya tatu utaiteketeza katika moto katikati ya jiji mara tu zitakapotimia siku za kuzingira.[e] Nawe utachukua sehemu nyingine ya tatu. Utaipiga kwa upanga kulizunguka jiji pande zote,[f] nayo sehemu ya tatu ya mwisho utaitawanya kwenye upepo, nami nitauchomoa upanga nyuma yao.[g]

3 "Nawe utachukua hesabu ndogo katika hizo na kuzifunga katika pindo za nguo yako.[h] **4** Na nyingine kati ya hizo utazichukua nawe utazitupa katikati ya moto na kuziteketeza katika moto. Kutoka kwa moto huo utatoka na kwenda katika nyumba yote ya Israeli.[i]

5 "Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema, 'Huyu ni Yerusalemu. Katikati ya mataifa nimemweka, kukiwa na nchi zinazomzunguka pande zote. **6** Naye alijiendesha kwa kuyaasi maamuzi yangu ya hukumu katika uovu kuliko mataifa,[j] na kuziasi sheria zangu kuliko nchi zinazomzunguka pande zote, kwa maana waliyakataa maamuzi yangu ya hukumu, nao hawakutembea katika sheria zangu.'[a]

7 "Kwa hiyo hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema, 'Kwa sababu mlikuwa na fujo[b] kuliko mataifa yanayowazunguka ninyi pande zote, hamkutembea katika sheria zangu na hamkufanya maamuzi yangu ya hukumu;[c] bali mlifanya kulingana na maamuzi ya hukumu ya mataifa yanayowazunguka pande zote, sivyo?[d] **8** kwa hiyo hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: "Tazama niko dhidi yako, Ee jiji, naam mimi,[e] nami nitayatenda katikati yako maamuzi ya hukumu machoni pa mataifa.[f] **9** Nami nitafanya ndani yako jambo ambalo sijafanya na ambalo mfano wake sitafanya tena kwa sababu ya machukizo yenu yote.[g]

10 "'"Kwa hiyo akina baba wenyewe watakula wana katikati yako,[h] na wana wenyewe watakula baba zao, nami nitatenda ndani yako matendo ya hukumu na kutawanya mabaki yako yote kuelekea kila upepo."'[i]

11 "'Kwa hiyo kama ninavyoishi,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'kwa hakika kwa sababu ni patakatifu pangu ulipopatia unajisi kwa machukizo[j] yako yote na kwa vinyaa[k] vyako vyote, mimi mwenyewe pia Ndiye nitakayekupunguza[l] wewe nalo jicho langu halitakusikitikia[m] na mimi mwenyewe sitakuhurumia.[n] **12** Sehemu ya tatu yako—kwa tauni watakufa,[o]

SURA 4
a 2Fa 25:3; Yer 37:21; Omb 1:11; Omb 4:9; Omb 5:9; Ufu 6:6
b Eze 12:18
c Law 26:39; Eze 24:23

SURA 5
d Law 21:5; Eze 44:20
e Yer 9:21; Eze 4:8
f Yer 15:2
g Law 26:33; Eze 12:14; Amo 9:1
h Yer 40:6; Yer 52:16
i Yer 4:4
j Kum 32:15; 2Fa 17:8; Eze 16:47

Safu ya 2
a Ne 9:16; Zb 78:10; Yer 8:5; Yer 11:10
b 2Fa 21:9; 2Nya 33:9
c Yer 44:23
d 2Fa 21:11; Yer 2:11; Eze 16:47
e Yer 21:5; Eze 15:7
f Kum 29:24; 1Fa 9:8; Omb 2:15
g Omb 4:6; Da 9:12; Amo 3:2
h Law 26:29; Kum 28:53; 2Fa 6:29; Yer 19:9; Omb 2:20; Omb 4:10
i Law 26:33; Kum 4:27; Kum 28:64; Ne 1:8; Eze 12:14; Eze 17:21
j Law 19:30; Law 20:3; 2Fa 21:7; 2Nya 36:14; Yer 32:34
k Kum 7:25; Yer 16:18; Eze 23:38
l Zb 107:39
m Kum 29:20; Eze 7:4; Eze 8:18
n Omb 2:21; Zek 11:6
o Yer 14:12; Eze 6:12

na kwa njaa watafikia mwisho
wao katikati yako.[a] Na sehemu
nyingine ya tatu—kwa upa-
nga wataanguka kukuzungu-
ka pande zote. Na sehemu ya
tatu ya mwisho nitawatawa-
nya hata kuelekea kila upe-
po,[b] nami nitauchomoa upanga
nyuma yao.[c] **13** Na hasira ya-
ngu hakika itafikia mwisho[d]
wake nami nitaituliza ghadha-
bu yangu juu yao[e] na kujifari-
ji mwenyewe;[f] nao watalazimi-
ka kujua kwamba mimi mwe-
nyewe, Yehova, nimesema kati-
ka kusisitiza kwangu kwamba
watu wajitoe kikamili,[g] nitaka-
pomaliza ghadhabu yangu juu
yao.

14 “‘Nami nitakufanya kuwa
ukiwa na shutuma kati ya mataifa
yanayokuzunguka pande zote
mbele ya macho ya kila mpita-
njia.[h] **15** Nawe utakuwa shu-
tuma[i] na kitu cha kutukanwa,[j]
mfano wa kuonya[k] na tisho kwa
mataifa yanayokuzunguka pa-
nde zote, nitakapotenda ndani
yako matendo ya hukumu kati-
ka hasira na katika ghadhabu
na katika makaripio ya ghadha-
bu.[l] Mimi mwenyewe, Yehova,
nimesema.

16 “‘Nitakapotuma ile mi-
shale yenye madhara ya njaa
juu yao,[m] itakayokuwa ya uha-
ribifu, mishale ambayo nita-
tuma ili kuwaharibu ninyi,[n]
hata njaa nitaiongeza juu yenu
nami nitazivunja fimbo zenu
ambazo mikate ya mviri-
ngo huning’inizwa kuzizungu-
ka.[o] **17** Nami nitatuma juu
yenu njaa na wanyama-mwi-
tu wenye kudhuru,[p] nao wa-
tawaua watoto wenu, na tau-
ni[q] na damu[r] zitapitia katika-
ti yenu, nami nitauleta upanga
juu yenu.[a] Mimi mwenyewe,
Yehova, nimesema.’”

6 Na neno la Yehova likae-
ndelea kunijia, na kusema:
2 “Mwana wa binadamu, ele-
keza uso wako kwenye milima
ya Israeli na uitolee unabii.[b]
3 Nawe utasema, ‘Enyi milima
ya Israeli, sikieni neno la Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova:[c]
Hivi ndivyo Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova ameiambia
milima na vilima,[d] vijito na
mabonde: “Tazama mimi! Ni-
naleta upanga juu yenu, nami
hakika nitaharibu mahali
penu pa juu.[e] **4** Na madhaba-
hu zenu zitafanywa ukiwa[f] na
vinara vyenu vya uvumba vi-
tavunjwa, nami nitawafanya
waliouawa kati yenu waangu-
ke mbele ya sanamu zenu za
mavi.[g] **5** Nami nitaiweka mi-
zoga ya wana wa Israeli mbele
ya sanamu zao za mavi, nami
nitaitawanya mifupa yenu ku-
zunguka pande zote za madha-
bahu zenu.[h] **6** Katika makao[i]
yenu yote majiji yataharibiwa[j]
na mahali pa juu patafanywa
ukiwa, ili padumu katika uha-
ribifu[k] na madhabahu zenu zi-
kae ukiwa na kuvunjwa[l] nazo
sanamu zenu za mavi zikome-
shwe[m] na vinara vyenu vya
uvumba vikatwe[n] na kazi zenu
zifutiliwe mbali. **7** Naye ali-
yeuawa hakika ataanguka ka-
tikati yenu,[o] nanyi mtalazimi-
ka kujua kwamba mimi ni Ye-
hova.[p]

8 “‘“Na wakati hilo litaka-
potukia nitawaruhusu muwe
na mabaki wale watakaoupo-
nyoka upanga kati ya mataifa,
wakati mtakapotawanywa
kati ya nchi mbalimbali.[q]
9 Na walioponyoka kati yenu

SURA 5
a Yer 15:2; Yer 21:9
b Yer 9:16
c Law 26:33; Yer 42:16; Eze 12:14
d Omb 4:11
e Eze 16:42
f Kum 32:36; Isa 1:24
g Kut 20:5; Kut 34:14; Kum 4:24; Kum 6:15; Yos 24:19; Isa 59:17; Eze 39:25
h Law 26:31; Kum 28:37; 1Fa 9:7; Ne 2:17
i Zb 79:4; Yer 24:9; Omb 2:15
j Omb 3:62
k 1Ko 10:11
l Eze 25:17
m Eze 14:21
n Kum 32:23; Zb 7:13
o Law 26:26; Eze 4:16; Eze 14:13
p Law 26:22; Kum 32:24; 2Fa 17:25; Eze 14:21; Eze 33:27
q Eze 38:22
r Eze 14:19

Safu ya 2
a Eze 21:3

SURA 6
b Eze 20:46; Eze 21:2; Eze 33:28; Eze 36:1
c Mik 6:2
d Yer 3:23; Yer 17:3
e Law 26:30
f Isa 27:9
g Law 26:30; 1Fa 13:2; Yer 16:18; Eze 8:10
h Yer 8:2
i Yer 9:19; Yer 32:29
j Isa 32:14; Yer 2:15; Mik 3:12
k Yer 17:3; Eze 16:39
l Ho 10:2
m Mik 1:7
n Isa 17:8
o Yer 14:18
p Eze 7:4
q Yer 30:10; Yer 44:28; Eze 14:22

hakika watanikumbuka kati
ya mataifa ambamo watakuwa
wamechukuliwa mateka,[a] kwa
kuwa nimevunjika moyo kwa
sababu ya moyo wao wenye ku-
fanya uasherati ambao ume-
geuka na kuniacha[b] na macho
yao yanayozifuata sanamu zao
za mavi katika uasherati;[c] na
nyuso zao hakika zitachuki-
zwa na mambo mabaya amba-
yo wamefanya katika machu-
kizo yao yote.[d] **10** Nao wata-
lazimika kujua kwamba mimi
ni Yehova; sikusema[e] kwa uba-
tili juu ya kuwatendea jambo
hili lenye msiba.”’[f]

11 “Hivi ndivyo Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova
amesema, ‘Piga makofi[g] na ku-
fanya vishindo kwa mguu
wako, na kusema: “Ole wa-
ngu!” kwa sababu ya machu-
kizo yote mabaya ya nyumba
ya Israeli,[h] kwa sababu wa-
taanguka[i] kwa upanga,[j] kwa
njaa[k] na kwa tauni. **12** Yule
aliye mbali,[l] kwa tauni ataku-
fa; na yule aliye karibu, kwa
upanga ataanguka; naye yule
aliyebaki na ambaye amelin-
dwa, kwa njaa atakufa, nami
nitaitimiza ghadhabu yangu
juu yao.[m] **13** Nanyi mtalazi-
mika kujua kwamba mimi ni
Yehova,[n] wakati ambapo walio-
uawa kati yao watakuwa kati-
kati ya sanamu zao za mavi,[o]
kuzunguka pande zote za ma-
dhabahu zao,[p] juu ya kila kili-
ma kirefu,[q] juu ya vilele vyote
vya milima[r] na chini ya kila mti
wenye majani mengi[s] na chi-
ni ya kila mti mkubwa wenye
matawi mengi,[t] mahali amba-
po wametoa harufu yenye ku-
tuliza kwa sanamu zao zote
za mavi.[u] **14** Nami nitaunyo-

SURA 6

a Kum 30:1
Zb 137:1
Eze 12:16
Zek 10:9
b Zb 78:40
Isa 7:13
Isa 63:10
c Hes 15:39
Eze 20:7
d Isa 64:6
Eze 20:43
Eze 36:31
e Isa 46:10
Isa 55:11
f Eze 14:23
Eze 33:29
Da 9:12
Zek 1:6
g Eze 21:14
h Yoe 1:15
i Yer 24:10
Eze 5:12
j Yer 15:2
k Yer 16:4
l Da 9:7
m Omb 4:22
Eze 5:13
n Eze 12:15
Eze 38:23
o Eze 6:4
p Yer 8:2
q Kum 12:2
Isa 65:7
Yer 2:20
Eze 20:28
r Yer 3:6
Ho 4:13
s 1Fa 14:23
t Isa 57:5
u Isa 65:3

Safu ya 2

a Isa 5:25

SURA 7

b Amo 8:2
c Eze 5:13
d Hes 32:23
Yer 40:3
Eze 18:30
Eze 33:20
Ro 2:6
e Yer 13:14
Eze 5:11
Eze 8:18
Eze 9:10
Zek 11:6
f Yer 16:18
Eze 11:21
Eze 16:43
g Eze 6:13
h 2Fa 21:12
Da 9:12
i Yer 44:27
j Eze 21:25
Eze 39:8
k Eze 12:23
Sef 1:14
l 2Nya 34:21
Eze 36:18
m Yer 7:20
n Ayu 34:11
Eze 18:30
Ga 6:7

osha mkono wangu juu yao[a] na
kuifanya nchi iwe mahame ye-
nye ukiwa, kuwa ukiwa mbaya
zaidi kuliko nyika inayoelekea
Dibla, katika makao yao yote.
Nao watalazimika kujua kwa-
mba mimi ni Yehova.’”

7 Na neno la Yehova likae-
ndelea kunijia, na kusema:
2 “Na wewe, Ee Mwana wa bi-
nadamu, hivi ndivyo Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova ame-
iambia nchi ya Israeli, ‘Mwisho,
ule mwisho, umekuja juu ya mi-
isho minne ya nchi.[b] **3** Sasa
mwisho uko juu yako,[c] nami
nitaipeleka hasira yangu juu
yako, nami nitakuhukumu ku-
lingana na njia zako[d] na kuleta
juu yako machukizo yako yote.
4 Na jicho langu halitakusiki-
tikia, wala sitakuwa na huru-
ma,[e] kwa maana juu yako nita-
zileta njia zako mwenyewe, na
katikati yako machukizo yako
mwenyewe yatakuja kuwamo;[f]
nanyi mtalazimika kujua kwa-
mba mimi ni Yehova.’[g]

5 “Hivi ndivyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amesema,
‘Msiba, msiba wa pekee,
tazama! unakuja.[h] **6** Mwisho
wenyewe lazima uje.[i] Lazima
ule mwisho uje; lazima huo ua-
mke kwa ajili yako. Tazama!
Unakuja.[j] **7** Lazima shada li-
kujie wewe, Ee mkaaji wa nchi,
wakati utakuja, siku ile iko ka-
ribu.[k] Kuna mvurugo, wala si
kupaaza sauti kwa milima.

8 “‘Hivi karibuni nitaimwa-
ga ghadhabu yangu juu yako,[l]
nami nitaitimiza hasira ya-
ngu juu yako,[m] nami nitakuhu-
kumu kulingana na njia zako[n]
na kuleta juu yako machuki-
zo yako yote. **9** Jicho langu

halitasikitika[a] wala sitakuonea huruma.[b] Kulingana na njia zako nitaleta juu yako, na machukizo yako mwenyewe yatakuja kuwa katikati yako;[c] nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova ninayewapiga.[d]

10 "'Tazama! Ile siku! Tazama! Inakuja.[e] Shada limetoka.[f] Fimbo imechanua.[g] Kimbelembele kimechipuka.[h] **11** Jeuri yenyewe imesimama na kuwa fimbo ya uovu.[i] Si kutoka kwao, wala kutoka kwa mali yao; na si kutoka kwao wenyewe, wala hamna ukuu wowote ndani yao. **12** Lazima wakati uje, siku ile lazima ifike. Mnunuzi na ashangilie;[j] naye muuzaji asianze kuomboleza, kwa maana kuna hasira juu ya umati wake wote. **13** Kwa maana kwa kile kilichouzwa muuzaji mwenyewe hatakirudia, uhai wao ukiwa bado katikati ya walio hai; kwa maana maono ni ya umati wake wote. Hakuna atakayerudi, na kila mmoja wao hatakuwa na uhai wake mwenyewe kupitia kwa kosa lake mwenyewe.

14 "'Wamepiga tarumbeta[k] na kila mtu ametayarishwa, lakini hakuna anayeenda kwenye pigano, kwa sababu hasira yangu iko juu ya umati wake wote.[l] **15** Upanga[m] uko nje, na tauni na njaa zimo ndani.[n] Yeyote aliye uwanjani, atakufa kwa upanga, na wowote walio jijini, njaa na tauni zitawameza.[o] **16** Na watu wao walioponyoka hakika wataponyoka[p] na kuwa kama njiwa wa mabondeni juu ya milima,[q] ambao wote wanaomboleza, kila mmoja katika kosa lake mwenyewe. **17** Nayo mikono yote, inaendelea kulegea;[a] nayo magoti yote yanaendelea kudondoka maji.[b] **18** Nao wamejifunga nguo za magunia,[c] na kutetemeka kumewafunika;[d] na nyuso zote zina aibu[e] na vichwa vyao vyote vina upara.[f]

19 "'Katika barabara watatupa fedha yao wenyewe, na dhahabu yao wenyewe itakuwa chukizo. Fedha yao wala dhahabu yao hazitaweza kuwakomboa katika siku ya ghadhabu ya Yehova.[g] Nafsi zao hawatazishibisha, nayo matumbo yao hawatayajaza, kwa maana ni kikwazo kinachosababisha kosa lao.[h] **20** Na pambo la mtu—mtu ameliweka kuwa sababu ya kiburi; na sanamu zao zenye kuchukiza,[i] machukizo[j] yao, wamezifanya kwa hilo. Ndiyo sababu nitalifanya hilo kuwa chukizo kwao.[k] **21** Nami nitalitia mkononi mwa wageni walipore na kuwapa waovu wa dunia liwe nyara,[l] nao hakika watalitia unajisi.

22 "'Nami nitaugeuzia mbali uso wangu kutoka kwao,[m] nao watapatia unajisi mahali pangu palipofichika, na wanyang'anyi wataingia ndani yake kwelikweli na kupatia unajisi.[n]

23 "'Fanya mnyororo,[o] kwa maana nchi yenyewe imejaa hukumu yenye madoa ya damu[p] na jiji lenyewe limejaa jeuri.[q] **24** Nami nitaingiza yaliyo mabaya kabisa kati ya mataifa,[r] nayo hakika yatazimiliki nyumba zao,[s] nami nitakikomesha kiburi cha wenye nguvu,[t] na patakatifu pao patatiwa unajisi.[u] **25** Kutakuwa na maumi-

SURA 7

a Yer 13:14
b Yer 15:5
c Eze 11:21
Eze 16:43
d Isa 66:6
Eze 33:29
e Sef 1:14
f Eze 7:7
g Isa 10:5
h Yer 50:31
i Isa 59:6
Yer 6:7
Mik 6:12
j Sef 1:18
k Yer 4:5
Yer 6:1
l Yer 7:20
Yer 12:12
m Law 26:25
n Kum 32:25
Yer 21:9
Yer 27:13
Omb 1:20
o Yer 14:18
Yer 15:2
Eze 5:12
p Ezr 9:15
Isa 1:9
Isa 37:31
Eze 6:8
q Isa 38:14
Isa 59:11
Nah 2:7

Safu ya 2

a Isa 13:7
Yer 6:24
b Eze 21:7
c Isa 3:24
Isa 15:3
Yer 48:37
Amo 8:10
d Zb 55:5
e Yer 3:25
f Isa 22:12
g Met 11:4
Sef 1:18
h Eze 14:3
Eze 44:12
i 2Fa 17:12
2Fa 21:7
Eze 6:4
j Yer 7:30
Yer 32:34
k Kum 27:15
Yer 7:14
Omb 1:17
Ho 9:10
l 2Nya 36:19
m Yer 18:17
n Kum 28:29
2Nya 36:19
Omb 1:10
o Yer 27:2
Yer 39:7
Yer 40:1
Omb 3:7
Nah 3:10
p 2Fa 21:16
2Fa 24:4
Yer 2:34
Yer 22:17
Eze 9:9
Eze 11:6
Ho 4:2
q Isa 59:6
Mik 2:2
r Kum 28:50
Eze 21:31
Hab 1:6
s Yer 6:12
Omb 5:2
t Isa 5:14
u Eze 21:2

vu makali, nao hakika watatafuta amani lakini hakutakuwa na yoyote.[a] **26** Shida itakuja juu ya shida,[b] na kutakuwa na habari juu ya habari, na hakika watu watatafuta maono kutoka kwa nabii,[c] na sheria yenyewe itaangamia kutoka kwa kuhani na shauri kutoka kwa wanaume wazee.[d] **27** Mfalme mwenyewe ataomboleza;[e] hata mkuu atajivika ukiwa,[f] na mikono yenyewe ya watu wa nchi itasumbuka. Kulingana na njia yao nitatenda kuwaelekea wao,[g] na kwa hukumu zao nitawahukumu wao;[h] nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.'"[i]

8 Na ikawa kwamba katika mwaka wa sita, katika mwezi wa sita, siku ya tano ya mwezi huo, nilikuwa nimeketi nyumbani mwangu nao wanaume wazee wa Yuda walikuwa wameketi mbele yangu,[j] mkono wa Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova uliponiangukia hapo.[k] **2** Nami nikaanza kuona, na, tazama! mfano unaoonekana kama moto;[l] kuanzia kuonekana kwa viuno vyake hata kuelekea chini kulikuwa na moto,[m] na kuanzia kuonekana kwa viuno vyake hata kuelekea juu kulikuwa na kitu kama kuonekana kwa mng'ao, kama mng'ao wa mchanganyiko wa dhahabu na fedha.[n] **3** Ndipo akanyoosha mfano wa mkono[o] na kuniinua kwa kishungi cha nywele za kichwa changu, na roho[p] ikanichukua katikati ya dunia na mbingu na kunileta Yerusalemu katika maono ya Mungu,[q] kwenye mwingilio wa lango la ndani[a] linaloelekea kaskazini, ambapo ni makao ya mfano wa wivu unaochochea wivu.[b] **4** Na, tazama! utukufu wa Mungu wa Israeli ulikuwa hapo,[c] kama kuonekana nilikokuwa nimeona katika nchi tambarare ya bondeni.

5 Naye akaniambia: "Mwana wa binadamu, tafadhali inua macho yako kuelekea upande wa kaskazini." Kwa hiyo nikayainua macho yangu kuelekea upande wa kaskazini, na, tazama! kaskazini mwa lango la madhabahu kulikuwa na mfano huu wa wivu[d] katika njia ya kuingilia. **6** Naye akaendelea kuniambia: "Mwana wa binadamu, je, unaona machukizo makubwa wanayofanya,[e] mambo ambayo nyumba ya Israeli wananifanyia hapa ili mimi niwe mbali na patakatifu pangu?[f] Na bado utaona tena machukizo makubwa."

7 Basi akanileta kwenye mwingilio wa ua, nami nikaanza kuona, na, tazama! tundu fulani ukutani. **8** Sasa akaniambia: "Mwana wa binadamu, toboa, tafadhali, ukutani."[g] Nami nikatoboa ukutani hatua kwa hatua, na, tazama! kulikuwa na mwingilio fulani. **9** Naye akazidi kuniambia: "Ingia ndani uone machukizo mabaya wanayoyafanya hapa."[h] **10** Kwa hiyo nikaingia na kuanza kuona, na, tazama! kulikuwa na kila mfano[i] wa vitu vyenye kutambaa na wanyama wenye kuchukiza,[j] na sanamu zote za mavi za nyumba ya Israeli,[k] michongo hiyo ikiwa juu ya ukuta kuuzunguka pande zote. **11** Na wanaume 70[l] wazee wa nyumba

SURA 7
a Isa 57:21; Yer 8:15
b Law 26:28; Kum 32:23; Yer 4:20
c Yer 21:2; Yer 37:17
d 1Fa 21:11; Zb 74:9; Yer 18:18; Omb 2:9; Eze 20:3
e Yer 52:10
f Eze 19:1
g Ayu 34:11; Ro 2:6
h Isa 3:11; Mt 7:2; Yak 2:13
i Eze 6:13

SURA 8
j Eze 14:1; Eze 20:1
k Eze 1:3; Eze 3:22
l Eze 1:27
m Da 7:9
n Eze 1:4; Eze 1:27
o Eze 2:9; Da 5:5
p Eze 3:14; Ebr 1:7
q Eze 40:2

Safu ya 2
a Yer 20:2; Eze 9:2
b Kut 20:5; Kum 32:16; Yos 24:19; Zb 78:58
c Kut 40:34; Eze 1:28
d Eze 7:20
e 2Nya 36:14
f Zb 78:60; Yer 26:6
g Yer 23:24; Ebr 4:13
h Yer 7:10
i Kut 20:4; Kum 4:18
j Law 11:10; Mdo 10:12; Ro 1:23
k 2Fa 23:24
l Kut 24:1; Hes 11:16

ya Israeli, pamoja na Yaazania mwana wa Shafani[a] akiwa amesimama kati yao, walikuwa wamesimama mbele ya hiyo, kila mmoja akiwa na chetezo chake mkononi mwake, na manukato ya wingu la uvumba yalikuwa yakipaa.[b]
12 Naye akaniambia: "Je, umeona, Ee mwana wa binadamu, mambo ambayo wazee wa nyumba ya Israeli wanafanya katika giza,[c] kila mmoja katika vyumba vya ndani vya sanamu yake ya kuchongwa? Kwa maana wanasema, 'Yehova hatuoni.[d] Yehova ameiacha nchi hii.'"

13 Naye akaendelea kuniambia: "Bado utaona tena machukizo makubwa wanayofanya."[e] **14** Kwa hiyo akanileta kwenye mwingilio wa lango la nyumba ya Yehova, linaloelekea kaskazini, na, tazama! wanawake walikuwa wameketi hapo, wakimlilia mungu Tamuzi.

15 Naye akazidi kuniambia: "Je, umeona hili, Ee mwana wa binadamu? Bado utaona tena machukizo[f] makubwa yaliyo mabaya kuliko haya." **16** Kwa hiyo akanileta katika ua wa ndani wa nyumba ya Yehova,[g] na, tazama! kwenye mwingilio wa hekalu la Yehova, katikati ya ukumbi na madhabahu,[h] kulikuwa na wanaume 25[i] hivi migongo yao ikielekea hekalu la Yehova[j] na nyuso zao zikielekea mashariki, nao walikuwa wameelekea mashariki, wakiliinamia jua.[k]

17 Naye akaendelea kuniambia: "Je, umeona hili, Ee mwana wa binadamu? Je, ni jambo dogo sana kwa nyumba ya Yuda kufanya machukizo ambayo wamefanya hapa, kwamba waijaze nchi jeuri[a] na kwamba wanitie uchungu tena, na tazama, wananyoosha lile chipukizi kuelekea pua yangu? **18** Na mimi mwenyewe pia nitachukua hatua katika ghadhabu.[b] Jicho langu halitasikitika, wala sitakuwa na huruma.[c] Nao hakika wataita masikioni mwangu kwa sauti kubwa, lakini sitawasikia."[d]

9 Naye akaita masikioni mwangu kwa sauti kubwa, na kusema: "Waleteni karibu wale wanaolikazia jiji fikira, kila mmoja wao akiwa na silaha yake mkononi mwake ili kuleta uharibifu!"

2 Na, tazama! kulikuwa na wanaume sita wakija kutoka upande wa lango la juu[e] linaloelekea kaskazini, kila mmoja akiwa na silaha yake ya kuponda mkononi mwake; na kulikuwa na mwanamume mmoja kati yao aliyevaa kitani,[f] akiwa na kidau cha wino kiunoni, nao wakaingia ndani na kusimama kando ya madhabahu ya shaba.[g]

3 Nao utukufu wa Mungu wa Israeli,[h] uliondolewa juu ya makerubi[i] ambao ulikuwa juu yao kwenye mlango wa nyumba hiyo,[j] naye akaanza kumwita yule mwanamume aliyevaa kitani,[k] ambaye alikuwa na kidau cha wino kiunoni. **4** Na Yehova akamwambia: "Pita katikati ya jiji, katikati ya Yerusalemu, nawe lazima utie alama kwenye mapaji ya uso ya watu wanaougua na kulia[l] kwa sababu ya machukizo yote yanayofanywa katikati yake."[m]

SURA 8
a 2Fa 22:3; 2Fa 25:22; 2Nya 34:8; Yer 26:24
b 2Nya 26:16; Yer 7:9; Eze 16:18
c Ayu 24:16; Yoh 3:19
d Zb 73:11; Zb 94:7; Isa 29:15; Eze 9:9
e Yer 9:3
f 2Nya 36:14
g 2Nya 4:9
h Yoe 2:17
i Eze 11:1
j 1Fa 8:29; Yer 2:27; Yer 32:33
k Kum 4:19; Kum 17:3; 2Fa 17:16; 2Fa 23:5; Ayu 31:26; Yer 8:2; Yer 44:17

Safu ya 2
a Mwa 6:13; 2Fa 21:16; Yer 19:4; Eze 9:9; Sef 1:9
b Eze 5:13
c Eze 5:11; Eze 7:9; Eze 9:10
d Met 1:28; Isa 1:15; Yer 11:11; Yer 14:12; Mik 3:4; Zek 7:13

SURA 9
e Yer 20:2; Eze 8:3
f Law 16:4
g 2Nya 4:1; 2Nya 7:7
h Eze 3:23; Eze 8:4; Eze 11:22
i Mwa 3:24
j Eze 10:4
k Ufu 19:8
l Zb 119:53; Zb 119:136; 2Ko 12:21; 2Pe 2:8
m Eze 5:11; Eze 8:6

5 Naye akawaambia hawa wengine masikioni mwangu: "Piteni katikati ya jiji nyuma yake na kupiga. Jicho lenu lisisikitike, wala msiwe na huruma yoyote.[a] **6** Mzee, kijana na bikira na mtoto mdogo na wanawake[b] mtawaua kabisa—mtawaharibu. Lakini mtu yeyote ambaye ana ile alama msimkaribie,[c] nanyi mnapaswa kuanzia patakatifu pangu."[d] Kwa hiyo wakaanza na wale wanaume wazee waliokuwa mbele ya nyumba.[e] **7** Naye akazidi kuwaambia: "Itieni nyumba unajisi na kuzijaza nyua kwa wale waliouawa.[f] Nendeni!" nao wakaenda na kupiga jijini.

8 Na ikawa kwamba, walipokuwa wakipiga nami nikiwa nimeachwa, nikaanguka kifudifudi,[g] nikapaaza kilio, na kusema: "Ole[h] wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Je, unawaharibu mabaki wote wa Israeli huku ukimwaga ghadhabu yako juu ya Yerusalemu?"[i]

9 Kwa hiyo akaniambia: "Kosa la nyumba ya Israeli na Yuda[j] ni kubwa, kubwa sana,[k] na nchi imejaa umwagaji wa damu[l] nalo jiji limejaa upotovu;[m] kwa maana wamesema, 'Yehova ameiacha nchi hii,[n] na Yehova haoni.'[o] **10** Na mimi pia, jicho langu halitasikitika,[p] wala sitaonyesha huruma.[q] Hakika nitaileta njia yao juu ya kichwa chao wenyewe."[r]

11 Na, tazama! yule mwanamume aliyevaa kitani, ambaye alikuwa na kidau cha wino kiunoni, akaleta neno, na kusema: "Nimefanya kama ulivyoniamuru."[s]

SURA 9

a Kut 32:27
Eze 7:4
b 2Nya 36:17
c Kut 12:23
Yos 2:18
Ufu 9:4
d 2Fa 25:18
Yer 25:29
1Pe 4:17
e Eze 8:11
f 2Nya 36:17
Omb 2:21
g Hes 14:5
Hes 16:45
h Yer 4:10
Eze 11:13
i Mwa 18:23
j Yer 11:10
k Kum 31:29
2Fa 17:7
2Nya 36:14
Isa 1:4
l 2Fa 21:16
Yer 2:34
Eze 24:9
Mt 23:30
m Eze 22:29
n Eze 8:12
o Zb 10:11
Isa 29:15
p Eze 7:4
Eze 8:18
q Eze 5:11
r Kum 32:41
2Nya 6:23
Eze 11:21
Ebr 10:30
s Mwa 6:22
Kut 39:32

Safu ya 2

SURA 10

a Eze 1:22
b Eze 1:26
Ufu 4:3
c Isa 6:1
Ufu 4:2
d Eze 9:2
e Eze 1:16
f Eze 1:13
g 2Fa 25:9
Zb 120:4
Zb 140:10
Ufu 8:5
h Eze 9:3
i Eze 1:28
j Kut 40:35
1Fa 8:10
2Nya 5:13
Eze 43:5
k Eze 1:24
Eze 11:22
l Zb 29:3
Yoh 12:28
Yoh 12:29
m Omb 2:4
Omb 4:11
n Eze 1:13

10 Nami nikaendelea kuona, na, tazama! juu ya anga[a] lililokuwa juu ya kichwa cha makerubi kulikuwa na kitu kama jiwe la yakuti,[b] kilichoonekana kama mfano wa kiti cha ufalme,[c] kikionekana juu yao. **2** Naye akamwambia yule mwanamume aliyevaa kitani,[d] akasema: "Ingia katikati ya magurudumu yanayozunguka,[e] upande wa ndani chini ya makerubi, ujaze mikono yako makaa[f] ya moto kutoka katikati ya makerubi na kuyatupa juu ya jiji."[g] Kwa hiyo akaingia ndani mbele ya macho yangu.

3 Nao makerubi walikuwa wamesimama upande wa kuume wa nyumba wakati mwanamume huyo alipoingia, nalo wingu lilikuwa limeujaza ua wa ndani.[h] **4** Na utukufu wa Yehova[i] ukainuka juu kutoka kwa makerubi mpaka kwenye mlango wa nyumba, nayo nyumba hiyo ikajaa wingu[j] hatua kwa hatua, na ua wenyewe ulikuwa umejaa wangavu wa utukufu wa Yehova. **5** Na sauti ya mabawa ya makerubi[k] ikasikiwa katika ua wa nje, kama sauti ya Mungu Mweza-Yote wakati anaposema.[l]

6 Na ikawa kwamba, alipomwamuru yule mwanamume aliyevaa kitani, na kusema: "Chukua moto kutoka katikati ya magurudumu yanayozunguka, kutoka katikati ya makerubi," akaingia na kusimama kando ya gurudumu. **7** Kisha kerubi yule akanyoosha mkono wake kutoka katikati ya makerubi mpaka kwenye moto[m] uliokuwa katikati ya makerubi,[n] akauchukua na

kuutia kwenye mikono ya yule mwanamume aliyevaa kitani,[a] naye akauchukua na kwenda nje. **8** Na kukaonekana katika makerubi hao mfano wa mkono wa mtu wa udongo chini ya mabawa yao.[b]

9 Nami nikaendelea kuona, na, tazama! kulikuwa na magurudumu manne kando ya makerubi, gurudumu moja kando ya kerubi mmoja na gurudumu moja kando ya kerubi mwingine,[c] na kuonekana kwa magurudumu hayo kulikuwa kama mng'ao wa jiwe la krisolito. **10** Na kuonekana kwao, yote manne yalikuwa mfano mmoja, kama vile gurudumu linavyokuwa katikati ya gurudumu.[d] **11** Yalipokuwa yakienda, yalikuwa yakienda pande zake nne. Hayakuwa yakigeuka yalipokuwa yakienda, kwa sababu mahali ambapo kichwa kingeelekea, yalienda huko. Hayakuwa yakigeuka yalipokuwa yakienda.[e] **12** Na mwili wao wote na migongo yao na mikono yao na mabawa yao na magurudumu yalijaa macho kuzunguka pande zote.[f] Hao wanne walikuwa na magurudumu yao. **13** Na kuhusu hayo magurudumu, yakaitwa masikioni mwangu, "Ee magurudumu yanayozunguka!"

14 Na kila mmoja wao alikuwa na nyuso nne.[g] Uso wa kwanza ulikuwa uso wa kerubi, na uso wa pili ulikuwa uso wa mtu wa udongo,[h] na wa tatu ulikuwa uso wa simba, na wa nne ulikuwa uso wa tai.[i]

15 Na makerubi hao walikuwa wakiinuka[j]—ni kiumbe hai kilekile nilichokuwa nimekiona kwenye mto Kebari[a]— **16** na makerubi hao walipoenda, magurudumu yale yalikuwa yakienda kando yao;[b] na makerubi hao walipoyainua mabawa yao yawe juu ya dunia, magurudumu yale hayakuwa yakibadili mwelekeo, kutoka kando yao.[c] **17** Wakati hawa waliposimama tuli, hayo yalisimama tuli; na wakati hawa walipoinuka,[d] hayo yaliinuka pamoja nao, kwa maana roho ya kile kiumbe hai ilikuwa ndani yao.[e]

18 Nao utukufu[f] wa Yehova ukatoka juu ya mlango wa nyumba na kusimama tuli juu ya makerubi.[g] **19** Nao makerubi sasa wakainua mabawa yao na kuinuka kutoka duniani[h] mbele ya macho yangu. Walipoenda, magurudumu yale pia yalikuwa karibu, kando yao; nao wakaanza kusimama katika mwingilio wa mashariki wa lango la nyumba ya Yehova, na utukufu wa Mungu wa Israeli ulikuwa juu yao, kutoka juu.

20 Hiki ndicho kiumbe hai[i] nilichokuwa nimeona chini ya Mungu wa Israeli kwenye mto Kebari,[j] hivyo nikajua kwamba walikuwa makerubi. **21** Nao wale wanne, kila mmoja wao alikuwa na nyuso nne[k] na kila mmoja alikuwa na mabawa manne, na mfano wa mikono ya mtu wa udongo ilikuwa chini ya mabawa yao. **22** Na mfano wa nyuso zao, zilikuwa nyuso zilezile ambazo mfano wake nilikuwa nimeuona kando ya mto Kebari.[l] Kila mmoja wao alikuwa akienda mbele moja kwa moja.[m]

SURA 10

a Eze 9:2
b Eze 1:8
c Eze 1:15
d Eze 1:16
e Eze 1:17
Eze 1:20
f Eze 1:18
Ufu 4:6
Ufu 4:8
g Eze 1:6
h Eze 1:10
Ufu 4:7
i Ufu 8:13
j Eze 11:22

Safu ya 2

a Eze 1:3
Eze 43:3
b Eze 1:19
c Eze 1:21
d Eze 1:20
e Ayu 27:3
f 1Fa 8:11
2Nya 7:3
Eze 1:28
Eze 9:3
g Eze 10:4
Eze 11:23
h Eze 11:22
i Eze 1:22
j Eze 1:1
k Eze 1:8
l Eze 1:10
m Eze 1:12
Eze 10:11

11 Na roho[a] ikaniinua juu[b]
na kunileta kwenye lango la mashariki la nyumba ya Yehova linaloelekea mashariki,[c] na, tazama! katika mwingilio wa lango kulikuwa na wanaume 25,[d] nami nikamwona katikati yao Yaazania mwana wa Azuri na Pelatia mwana wa Benaya, wakuu wa watu.[e] **2** Kisha akaniambia: "Mwana wa binadamu, hawa ndio wanaume wanaopanga hila ya madhara na kutoa mashauri mabaya juu ya jiji hili;[f] **3** ambao wanasema, 'Je, ujenzi wa nyumba haujakaribia?[g] Yeye ni chungu cha kupikia chenye mdomo mpana,[h] na sisi ni nyama.'

4 "Kwa hiyo toa unabii juu yao. Toa unabii, Ee mwana wa binadamu."[i]

5 Ndipo roho ya Yehova ikaniangukia,[j] naye akaendelea kuniambia: "Sema, 'Hivi ndivyo Yehova amesema:[k] "Ninyi mlisema jambo lililo sawa, Ee nyumba ya Israeli; na kuhusu mambo yanayokuja katika roho yenu, mimi mwenyewe nimeyajua.[l] **6** Mmewafanya waliouawa kati yenu katika jiji hili kuwa wengi, nanyi mmezijaza barabara zake kwa watu waliouawa."'"[m] **7** "Kwa hiyo hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema, 'Kuhusu wale waliouawa ambao ninyi mmewaweka katikati yake, wao ni nyama,[n] na yeye ndiye chungu cha kupikia chenye mdomo mpana;[o] na ninyi wenyewe mtatolewa katikati yake.'"[p]

8 "'Ninyi mmeuogopa upanga,[q] nami nitauleta upanga juu yenu,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.[a] **9** 'Nami hakika nitawatoa ninyi katikati yake na kuwatia mkononi mwa wageni[b] na kutekeleza juu yenu matendo ya hukumu.[c] **10** Kwa upanga mtaanguka.[d] Katika mpaka wa Israeli[e] nitawahukumu ninyi; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.[f] **11** Yeye mwenyewe hatakuwa kwenu chungu cha kupikia chenye mdomo mpana,[g] nanyi wenyewe hamtakuwa nyama katikati yake. Katika mpaka wa Israeli nitawahukumu ninyi, **12** nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova, kwa sababu hamkutembea katika masharti yangu na hamkuzitenda hukumu zangu,[h] bali mmetenda kulingana na hukumu za mataifa yanayowazunguka.'"[i]

13 Na ikawa kwamba mara tu nilipotoa unabii Pelatia mwana wa Benaya mwenyewe akafa,[j] nami nikaanguka kifudifudi, nikalia kwa sauti kubwa[k] na kusema: "Ole wangu, Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova![l] Je, utaangamiza mabaki ya Israeli?"[m]

14 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **15** "Mwana wa binadamu, kuhusu ndugu zako,[n] ndugu zako, wanaume wanaohangaikia haki yako ya kukomboa, na nyumba yote ya Israeli, yote kabisa, ndio ambao wakaaji wa Yerusalemu wamewaambia, 'Nendeni mbali kutoka kwa Yehova. Ni yetu; tumepewa nchi tuimiliki';[o] **16** kwa hiyo sema, 'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: "Ijapokuwa nimewaweka mbali kabisa katikati

SURA 11

a Ebr 1:7
b Eze 3:12
Eze 8:3
2Ko 12:2
c Eze 10:19
d Eze 8:16
e Isa 1:23
Eze 22:27
Ho 5:10
f Isa 30:1
Mik 2:1
g Eze 12:22
2Pe 3:4
h Yer 1:13
Eze 24:3
i Isa 58:1
Eze 3:17
Eze 20:46
Eze 21:2
j Hes 11:25
1Sa 10:6
Eze 2:2
Eze 3:24
Mik 3:8
2Pe 1:21
k 1Fa 22:14
Yer 1:7
l Eze 20:32
Ebr 4:13
m 2Fa 21:16
Yer 2:34
Eze 7:23
Eze 22:4
Mt 23:35
n Mik 3:3
o Yer 1:13
Eze 24:6
p Yer 52:27
q Yer 38:19
Yer 42:14

Safu ya 2

a Yer 44:12
1Th 2:16
b Kum 28:36
Zb 106:41
Yer 39:6
c Eze 5:8
Eze 16:41
Yud 15
d 2Fa 25:21
2Nya 36:17
Yer 52:10
e 1Fa 8:65
2Fa 14:25
Yer 52:27
f Zb 9:16
Eze 6:13
g Yer 1:13
h Kut 19:8
Law 26:40
1Fa 11:33
Ezr 9:7
Ne 9:34
Eze 20:16
i Kum 12:30
2Fa 21:2
2Nya 28:3
Zb 106:35
Eze 8:10
j Met 6:15
Mdo 5:5
k Zb 119:120
l Eze 9:8
m Kum 9:19
n Isa 66:5
o Eze 33:24

ya mataifa, na ijapokuwa nimewatawanya katikati ya nchi[a] hata hivyo nitakuwa patakatifu kwao kwa kitambo kidogo katikati ya nchi ambazo wameenda.”’[b]

17 “Kwa hiyo sema, ‘Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: “Pia nitawakusanya ninyi kutoka kwa vikundi vya watu na kuwakusanya ninyi kutoka katika nchi ambazo katikati yake mmetawanywa, nami nitawapa ninyi udongo wa Israeli.[c] **18** Nao hakika watakuja huko na kuondoa machukizo yake yote na vinyaa vyake vyote kutoka ndani yake.[d] **19** Nami nitawapa moyo mmoja,[e] nami nitaweka roho mpya ndani yao;[f] nami hakika nitauondoa ule moyo wa jiwe kutoka katika mwili[g] wao na kuwapa moyo wa nyama,[h] **20** ili watembee katika sheria zangu na kushika maamuzi yangu ya hukumu na kuyatenda;[i] na ili wawe watu wangu kwelikweli[j] na ili mimi mwenyewe niwe Mungu wao.”’[k]

21 “‘“Lakini kwa wale ambao moyo wao unatembea katika machukizo yao na vinyaa vyao,[l] hakika nitaleta njia yao wenyewe juu ya vichwa vyao,” asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.’”[m]

22 Na sasa wale makerubi[n] wakayainua mabawa yao, na yale magurudumu yalikuwa karibu nao,[o] nao utukufu[p] wa Mungu wa Israeli ulikuwa juu yao, kutoka juu.[q] **23** Nao utukufu wa Yehova[r] ukapaa kutoka juu katikati ya jiji na kuanza kusimama juu ya mlima[s] ulio upande wa mashariki wa jiji hilo.[a] **24** Na roho[b] ikaniinua[c] na mwishowe ikanileta Ukaldayo kwa watu waliohamishwa,[d] katika maono kwa roho ya Mungu; na yale maono niliyokuwa nimeyaona yakapaa kutoka juu yangu. **25** Nami nikaanza kuwaambia watu waliohamishwa mambo yote ya Yehova ambayo alikuwa amenifanya niyaone.[e]

12 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** “Mwana wa binadamu, unakaa katikati ya nyumba yenye kuasi,[f] ambao wana macho ya kuona lakini kwa kweli hawaoni,[g] ambao wana masikio ya kusikia lakini kwa kweli hawasikii,[h] kwa maana wao ni nyumba yenye kuasi.[i] **3** Na wewe, Ee mwana wa binadamu, jifanyie mizigo kwa ajili ya uhamisho nawe uende uhamishoni wakati wa mchana mbele ya macho yao, nawe utaenda uhamishoni kutoka mahali pako mpaka mahali pengine mbele ya macho yao. Labda wataona, ingawa wao ni nyumba yenye kuasi.[j] **4** Nawe utatoa nje mizigo yako kama mizigo ya uhamisho wakati wa mchana mbele ya macho yao, na wewe mwenyewe utatoka nje wakati wa jioni mbele ya macho yao kama wale wanaotolewa ili kupelekwa uhamishoni.[k]

5 “Mbele ya macho yao, toboa njia yako ukutani, nawe utaitolea hapo.[l] **6** Mbele ya macho yao utaibeba begani. Wakati wa giza utaitoa nje. Utaufunika uso wako usiione dunia, kwa sababu nimekufanya kuwa ishara[m] kwa nyumba ya Israeli.”[n]

SURA 11
a Law 26:44
Kum 30:3
2Fa 24:15
Zb 44:11
Yer 24:5
Yer 30:11
Yer 31:10
b Zb 31:20
Zb 90:1
Zb 91:9
Met 18:10
c Isa 11:11
Yer 30:10
Yer 32:37
Eze 20:42
Eze 34:13
Eze 36:24
Eze 37:12
Amo 9:14
d Eze 37:23
e 2Nya 30:12
Yer 24:7
Yer 32:39
f Zb 51:10
Yer 31:33
Yer 32:39
Eze 36:31
Efe 4:23
g Isa 48:4
Zek 7:12
Mk 10:5
Ro 2:5
h Eze 36:26
i Zb 105:45
j Yer 11:4
k Eze 14:11
l Yer 17:9
m Eze 9:10
Eze 22:31
n Eze 9:3
Eze 10:2
o Eze 1:19
Eze 10:19
p 1Fa 8:11
2Nya 7:3
q Eze 10:18
r Eze 8:4
Eze 9:3
Eze 10:4
Eze 43:4
s Zek 14:4
Mt 24:3
Mdo 1:12

Safu ya 2
a Eze 43:2
b Eze 8:3
Ebr 1:7
c 2Ko 12:2
d Zb 137:1
e Eze 2:7

SURA 12
f Eze 2:3
Eze 3:26
g Isa 6:9
Isa 44:18
Mt 13:13
h Yer 5:21
Ro 11:8
i Eze 2:5
j Isa 1:2
k 2Nya 36:20
Yer 52:11
l 2Fa 25:4
Yer 39:4
m Eze 24:24
n Isa 8:18
Eze 4:3
Eze 12:3

7 Nami nikafanya vile nilivyokuwa nimeamriwa.[a] Mizigo yangu nikaitoa nje, kama vile mizigo ya kwenda uhamishoni, wakati wa mchana; na jioni nikatoboa njia yangu ukutani kwa mkono. Wakati wa giza nikaitoa nje. Nikaibeba juu ya bega langu, mbele ya macho yao.

8 Na neno la Yehova likaendelea kunijia asubuhi, na kusema: **9** "Mwana wa binadamu, je, wale wa nyumba ya Israeli, nyumba yenye kuasi,[b] hawakukuambia, 'Unafanya nini?' **10** Waambie, 'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: "Kuhusu mkuu,[c] kuna tangazo hili juu ya Yerusalemu na nyumba yote ya Israeli walio katikati yao."'

11 "Sema, 'Mimi ni ishara[d] kwenu. Kama vile nilivyotenda, ndivyo watakavyotendewa. Wataenda uhamishoni, utekwani.[e] **12** Na kuhusu mkuu aliye katikati yao, atabeba begani wakati wa giza na kutoka nje; watautoboa ukuta ili kuitolea hapo.[f] Uso wake ataufunika ili asiione dunia kwa jicho lake mwenyewe.' **13** Nami nitautandaza wavu wangu juu yake, naye atakamatwa katika wavu wangu wa kuwindia;[g] nami nitampeleka Babiloni, mpaka nchi ya Wakaldayo,[h] lakini hataiona; naye atakufa huko.[i] **14** Na wote wanaomzunguka ili kumsaidia, na majeshi yake yote, nitawatawanya kuelekea kila upepo;[j] na upanga nitauchomoa nyuma yao.[k] **15** Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapowatawanya katikati ya mataifa nami kwa kweli niwatawanye katikati ya nchi hizo.[a] **16** Na kati yao nitaacha watu wachache waponyoke upanga,[b] njaa na tauni, ili wayasimulie machukizo[c] yao yote katikati ya mataifa ambamo wataingia ndani yake;[d] nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova."

17 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **18** "Mwana wa binadamu, utakula mkate wako kwa kutetemeka, nawe utakunywa maji yako kwa kufadhaika na kwa kuhangaika.[e] **19** Nawe utawaambia watu wa nchi, 'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amewaambia wakaaji wa Yerusalemu katika udongo wa Israeli:[f] "Watakula mkate wao kwa hangaiko, nao watakunywa maji yao kwa tisho, ili kujaa kwa nchi yao kufanywe kuwa ukiwa[g] kwa sababu ya jeuri ya wale wote wanaokaa ndani yake.[h] **20** Nayo majiji yanayokaliwa yatakuwa ukiwa,[i] na nchi yenyewe itakuwa mahame yenye ukiwa;[j] nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova."'"[k]

21 Nalo neno la Yehova likazidi kunijia, na kusema: **22** "Mwana wa binadamu, ni neno gani hili la kimethali mlilo nalo katika udongo wa Israeli,[l] linalosema, 'Siku zimerefushwa,[m] na maono yote yameangamia'?[n] **23** Kwa hiyo waambie, 'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: "Hakika nitalifanya neno hili la kimethali likome, nao hawatalisema tena kama methali katika Israeli."'[o] Lakini waambie, 'Siku zimekaribia,[p] na jambo linalohusu

SURA 12

a Mwa 6:22
Kut 39:32
b Kum 31:27
Ne 9:26
Zb 78:8
Eze 3:9
Eze 24:3
c Yer 21:7
Eze 21:25
d Eze 24:24
e Yer 15:2
Yer 20:6
Yer 44:30
Yer 52:15
f 2Fa 25:4
Yer 39:4
Yer 52:7
g Ayu 19:6
Zb 66:11
Yer 52:9
Omb 1:13
Eze 17:20
Eze 19:8
Eze 32:3
Ho 5:1
Ho 7:12
Lu 21:35
h Yer 24:5
i 2Fa 25:7
Yer 34:3
Yer 39:7
Yer 52:11
Eze 17:16
j 2Fa 25:5
Eze 5:10
Eze 17:21
k Law 26:33
Yer 42:16

Safu ya 2

a Zb 9:16
Eze 6:14
b Isa 1:9
Isa 10:22
Eze 6:8
Ro 9:27
c Yer 44:22
Eze 6:11
Eze 7:3
Eze 33:29
d Law 26:41
e Law 26:26
Zb 80:5
f Eze 18:2
Eze 21:3
g Isa 6:11
Zek 7:14
h Zb 107:34
Yer 6:7
i Isa 64:10
Yer 25:9
j Isa 7:24
Yer 4:23
k Eze 6:13
l Eze 18:2
m Isa 5:19
Amo 6:3
n 2Pe 3:4
o Isa 28:22
Eze 18:3
p Yoe 2:1
Sef 1:14

maono yote.’ **24** Kwa maana hakutakuwako tena maono yoyote yasiyo na thamani[a] wala uaguzi wenye nyuso mbili katikati ya nyumba ya Israeli.[b] **25** ‘“Kwa maana mimi mwenyewe, Yehova, nitasema neno nitakalosema, nalo litafanywa.[c] Hakutakuwa na kucheleweshwa tena,[d] kwa maana katika siku zenu,[e] Ee nyumba yenye kuasi, nitasema neno na kulifanya hakika,” asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.’”

26 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **27** “Mwana wa binadamu, tazama! Wale wa nyumba ya Israeli wanasema, ‘Maono anayoona ni ya siku nyingi zinazokuja, naye anatoa unabii kuhusu nyakati zilizo mbali.’[f] **28** Kwa hiyo waambie, ‘Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema:’ “‘Hakutakuwa na kucheleweshwa tena kwa yoyote ya maneno yangu.[g] Neno nitakalosema, litafanywa,’[h] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.’”’”[i]

13 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** “Mwana wa binadamu, toa unabii kuwahusu manabii wa Israeli wanaotoa unabii,[j] nawe utawaambia wale wanaotoa unabii kutoka moyoni mwao wenyewe,[k] ‘Sikieni neno la Yehova.[l] **3** Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: “Ole wao manabii wajinga,[m] wanaoifuata roho yao wenyewe,[n] wakati ambapo hakuna chochote ambacho wameona![o] **4** Kama mbweha katika mahali palipo ukiwa ndivyo manabii wako mwenyewe wamekuwa, Ee Israeli.[a] **5** Hakika ninyi hamtaingia katika mapengo,[b] wala hamtajenga ukuta wa mawe[c] kwa ajili ya nyumba ya Israeli, ili kusimama vitani katika ile siku ya Yehova.”[d] **6** “Wameona maono ya jambo lisilo la kweli na uaguzi wa uwongo,[e] wale wanaosema, ‘Neno la Yehova ni,’ wakati ambapo Yehova mwenyewe hajawatuma, nao wamengoja neno litimie.[f] **7** Je, ninyi hamkuona maono yasiyo ya kweli, na kusema uaguzi wa uwongo, mnaposema, ‘Neno la Yehova ni,’ wakati ambapo mimi mwenyewe sikusema lolote?”’[g]

8 “‘Kwa hiyo hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: “‘Kwa sababu ninyi mmesema mambo yasiyo ya kweli na kuona uwongo, kwa hiyo tazama mimi niko dhidi yenu,’[h] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.” **9** Na mkono wangu umekuwa dhidi ya manabii wanaoona mambo yasiyo ya kweli na wanaoagua uwongo.[i] Katika kikundi cha rafiki wa karibu[j] wa watu wangu hawataendelea kukaa, nao hawataandikwa katika kitabu cha kuandikisha cha nyumba ya Israeli,[k] na katika udongo wa Israeli hawatakuja;[l] nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ndiye Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova,[m] **10** kwa sababu, naam, kwa sababu wamewapotosha watu wangu, na kusema, “Kuna amani!” wakati hakuna amani,[n] pia kuna mtu anayejenga ukuta wa kugawanya, lakini kwa ubatili[o]

SURA 12
a Eze 13:23
b 1Fa 22:11
Yer 14:14
Omb 2:14
c Isa 14:24
Isa 55:11
Omb 2:17
Da 9:12
Zek 1:6
d Ufu 10:6
e Yer 16:9
Hab 1:5
f Isa 5:19
Isa 28:15
2Pe 3:4
g Yer 44:28
Ga 4:4
Ufu 10:6
h Yos 23:14
Isa 46:10
Isa 55:11
i Eze 2:4

SURA 13
j Mik 3:5
Sef 3:4
2Pe 2:1
k Yer 14:14
Yer 23:16
l Amo 7:16
m Met 28:26
n Zb 81:12
o Yer 23:32

Safu ya 2
a Wim 2:15
Ga 2:4
Efe 4:14
b Zb 106:23
c Eze 22:30
d Isa 2:12
Yoe 1:15
e Eze 12:24
f Yer 29:31
g 2Pe 2:1
h Eze 21:3
Eze 22:28
i Yer 14:14
Yer 28:16
Yer 29:9
j Zb 111:1
k Kut 32:32
Ne 7:5
Zb 69:28
l Eze 20:38
m Eze 6:13
Eze 11:10
n Isa 57:21
Yer 6:14
Yer 8:11
o Zb 127:1

kuna wale wanaoupiga lipu
kwa chokaa.’[a]
11 “Waambie wale wanaopi-
ga lipu kwa chokaa kwamba
huo utaanguka. Mvua kubwa
yenye kufurika hakika itaku-
ja, na ninyi, enyi mawe ya mvua,
mtaanguka, na mlipuko wa dho-
ruba utasababisha mpasuko.[b]
12 Na, tazama! ukuta huo la-
zima utaanguka. Je, ninyi ha-
mtaambiwa, ‘Uko wapi mpako
ambao mliupiga lipu?’[c]
13 “Kwa hiyo hivi ndivyo
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova amesema, ‘Pia nitasaba-
bisha mlipuko wa dhoruba uli-
puke katika ghadhabu yangu,
na katika hasira yangu kuta-
tukia mvua yenye kufurika,
na katika ghadhabu kutaku-
wa na mawe ya mvua kwa ajili
ya maangamizi.[d] **14** Nami ni-
taubomoa ukuta ambao ninyi
mmeupiga lipu kwa chokaa na
kuuangusha chini, nao msingi
wake utafunuliwa.[e] Naye haki-
ka ataanguka, nanyi mtafikia
mwisho katikati yake; nanyi
mtalazimika kujua kwamba
mimi ni Yehova.’[f]
15 “‘Nami nitaimalizia gha-
dhabu yangu juu ya ukuta huo
na juu ya wale wanaoupiga
lipu kwa chokaa, nami nita-
waambia ninyi: “Ukuta hau-
ko tena, na wale wanaoupiga
lipu hawako tena,[g] **16** mana-
bii wa Israeli wanaotoa unabii
kwa Yerusalemu na ambao wa-
namwonea maono ya amani,[h]
wakati hakuna amani,”’ asema
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova.[i]
17 “Na wewe, Ee mwana wa
binadamu, elekeza uso[j] wako
juu ya binti za watu wako wa-
naotenda kama manabii[k] kuto-

SURA 13
a 2Nya 18:12
Isa 30:10
Eze 22:28
b Isa 25:4
Isa 27:8
Eze 38:22
c Yer 37:19
d Hag 2:17
e Mik 1:6
Mt 7:27
f Eze 14:8
g Isa 30:13
h Yer 6:14
Yer 28:9
i Isa 48:22
j Eze 20:46
Eze 21:2
k Kut 15:20
2Fa 22:14
Lu 2:36

Safu ya 2
a Ufu 2:20
b Eze 22:25
2Pe 2:14
c Met 28:21
Mik 3:11
d 1Fa 21:15
e Yer 23:14
Lu 6:26
f Ho 9:8
g Zb 9:16
Eze 6:13
h Yer 27:14
i Yer 23:14

kana na moyo wao wenyewe,[a]
utoe unabii juu yao. **18** Nawe
utasema, ‘Hivi ndivyo Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova
amesema: “Ole wao wanawake
wanaoshona pamoja tepe juu
ya viwiko vyote vya mkono
na kufanya ushungi juu ya ki-
chwa cha kila ukubwa ili ku-
winda nafsi!”[b] Je, nafsi amba-
zo ninyi wanawake mnawinda
ni zile za watu wangu, nazo
nafsi zenu ndizo mnazohifadhi
hai? **19** Na je, mtanitia una-
jisi mimi kuelekea watu wa-
ngu kwa ajili ya makonzi ya
shayiri na kwa ajili ya vipande
vya mkate,[c] ili kuziua nafsi zi-
sizopaswa kufa[d] na ili kuzihi-
fadhi hai nafsi zisizopaswa ku-
ishi kwa uwongo wenu mnao-
waambia watu wangu, wanao-
usikia uwongo?”’[e]
20 “Kwa hiyo hivi ndivyo
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova amesema, ‘Tazama, mimi
niko dhidi ya tepe zenu ni-
nyi wanawake, ambazo mnatu-
mia kuwinda nafsi kana
kwamba ni vitu vinavyoruka,
nami nitazipasua kutoka mi-
kononi mwenu na kuzifungu-
lia nafsi mnazowinda, nafsi
kana kwamba ni vitu vina-
vyoruka.[f] **21** Nami nitapa-
sua ushungi wenu na kuwako-
mboa watu wangu kutoka ka-
tika mkono wenu, nao hawa-
takuwa tena windo mkononi
mwenu; nanyi mtalazimika ku-
jua kwamba mimi ni Yehova.[g]
22 Kwa sababu kupitia uwo-
ngo mnauhuzunisha moyo wa
aliye mwadilifu,[h] wakati mimi
mwenyewe sikuwa nimemsa-
babishia maumivu, na kwa ku-
ifanya mikono ya aliye mwo-
vu kuwa yenye nguvu[i] hivi

kwamba asigeuke na kuiacha
njia yake mbaya ili kumhi-
fadhi hai,[a] **23** kwa hiyo ni-
nyi wanawake hamtaendelea
kuona maono yasiyo ya kwe-
li,[b] na uaguzi[c] ninyi hamta-
ufanya[d] tena;[e] nami nitawako-
mboa watu wangu kutoka kati-
ka mkono wenu,[f] nanyi mtala-
zimika kujua kwamba mimi ni
Yehova.'"[g]

14 Na wanaume kati ya wa-
zee wa Israeli wakani-
jia na kuketi mbele yangu.[h]
2 Ndipo neno la Yehova lika-
nijia, na kusema: **3** "Mwana
wa binadamu, kuhusu wana-
ume hawa, wameleta sanamu
zao za mavi juu ya mioyo yao,
na kikwazo kinachosababisha
kosa lao wamekiweka mbe-
le ya nyuso zao.[i] Je, watau-
liza hata kidogo juu yangu?[j]
4 Basi sema nao, nawe uta-
waambia, 'Hivi ndivyo Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova
amesema: "Mtu yeyote wa nyu-
mba ya Israeli anayeleta sana-
mu zake za mavi[k] juu ya moyo
wake na ambaye anaweka ki-
kwazo kinachosababisha kosa
lake mbele ya uso wake na ku-
mwendea nabii, mimi, Yehova,
nitakubali kuletwa ili nimjibu
katika habari hiyo kulingana
na wingi wa sanamu zake za
mavi,[l] **5** kwa kusudi la kui-
kamata nyumba ya Israeli kwa
moyo wao,[m] kwa sababu wao
wenyewe wamejiondoa kwa-
ngu kupitia kwa sanamu zao
za mavi—zote hizo."'[n]

6 "Kwa hiyo iambie nyumba
ya Israeli, 'Hivi ndivyo Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yeho-
va amesema: "Rudini, mgeuke
na kuziacha sanamu zenu za
mavi[o] na mgeuze nyuso zenu
kutoka kwa machukizo yenu
yote;[a] **7** kwa maana mtu ye-
yote kutoka katika nyumba ya
Israeli au kutoka kati ya waka-
aji wageni wanaokaa wakiwa
wageni katika Israeli, anaye-
jiondoa mwenyewe asinifuate[b]
na anayeleta sanamu zake za
mavi juu ya moyo wake na ku-
weka kikwazo kinachosababi-
sha kosa mbele ya uso wake na
ambaye anamjia nabii ili kuuli-
za habari kwa ajili yake mwe-
nyewe kupitia kwangu, mimi,[c]
Yehova, mimi mwenyewe nina-
kubali kumjibu. **8** Nami ni-
tauelekeza uso wangu juu ya
mtu huyo[d] na kumweka awe
ishara[e] na maneno ya kime-
thali,[f] nami nitamkatilia mba-
li kutoka katikati ya watu wa-
ngu;[g] nanyi mtalazimika kujua
kwamba mimi ni Yehova."'[h]

9 "'Naye nabii, ikiwa ata-
pumbazwa naye hakika ase-
me neno, mimi mwenyewe,
Yehova, nimempumbaza na-
bii huyo;[i] nami nitaunyoosha
mkono wangu juu yake na
kumwangamiza kutoka kati-
kati ya watu wangu Israeli.[j]
10 Nao lazima watalibeba kosa
lao.[k] Kosa la mwenye kuuliza
litakuwa kama kosa la nabii,[l]
11 ili wale wa nyumba ya Isra-
eli wasiweze tena kutanga-ta-
nga na kuacha kunifuata[m] wala
wasijichafue tena kwa mako-
sa yao yote. Nao watakuwa
watu wangu na mimi mwenye-
we nitakuwa Mungu wao,' ase-
ma Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova."[n]

12 Nalo neno la Yehova li-
kaendelea kunijia, na kusee-
ma: **13** "Mwana wa binada-
mu, kwa habari ya nchi, ikiwa
itanitendea dhambi kwa kute-

SURA 13

a Yer 23:17
2Pe 2:18
b Met 12:19
c Kum 18:10
Yer 27:9
d Kum 18:14
Isa 44:25
e Eze 12:24
Mik 3:6
f Eze 34:10
2Pe 2:9
g Eze 14:8

SURA 14

h Eze 8:1
Eze 20:1
Eze 33:31
i Eze 7:19
Ufu 2:14
j 2Fa 3:13
Isa 1:15
Yer 11:11
Zek 7:13
k Eze 6:4
l 2Fa 1:16
Isa 66:4
m Ho 10:2
Zek 7:12
Ebr 3:12
n Kum 32:16
Yer 2:5
o 1Sa 7:3
1Fa 8:47
Isa 55:7
Yer 8:5
Mdo 3:19

Safu ya 2

a Isa 30:22
Yer 13:27
b Isa 59:13
Yer 17:5
c Yer 21:2
Eze 33:31
d Law 17:10
Yer 44:11
Eze 15:7
e Hes 26:10
f Kum 28:37
Yer 24:9
g Law 20:3
h Eze 6:7
i 1Fa 22:22
Yer 4:10
2Th 2:11
j Isa 5:25
Isa 9:17
k Eze 3:18
Ro 1:27
l Yer 14:16
m Kum 13:11
2Pe 2:15
n Mwa 17:7
Yer 24:7
Eze 11:20
Eze 37:27
Ebr 8:10

nda kwa kukosa uaminifu,[a] pia
nitaunyoosha mkono wangu
juu yake na kuivunjia fimbo
ambazo mikate ya mviringo
huning'inizwa,[b] nami nitaleta
njaa[c] juu yake na kumkatilia
mbali mtu wa udongo na mnya-
ma wa kufugwa kutoka ndani
yake."[d] **14** "'Na kama watu
hawa watatu wangekuwa kati-
kati yake, Noa,[e] Danieli[f] na
Ayubu,[g] wao wenyewe kwa sa-
babu ya uadilifu[h] wao wangei-
komboa nafsi yao,' asema Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova."[i]
15 "'Au nikipitisha wanya-
ma-mwitu wenye kudhuru
nchini[j] nao wawaue watoto[k]
wenu nayo nchi iwe mahame
yenye ukiwa bila mtu yeyo-
te anayeipitia kwa sababu ya
wanyama-mwitu,[l] **16** kama
watu hao watatu wangekuwa
katikati yake, kama ninavyo-
ishi,' asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova, 'hawangeko-
mboa wana wala mabinti; wao,
wao wenyewe tu, ndio wange-
kombolewa nayo nchi ingeku-
wa mahame yenye ukiwa.'"[m]
17 "'Au kama ningeuleta
upanga juu ya nchi hiyo,[n] nami
niseme: "Upanga wenyewe upi-
te katikati ya nchi," nami ni-
mkatilie mbali mtu wa udo-
ngo na mnyama wa kufugwa,[o]
18 hata kama watu hawa wata-
tu wangekuwa katikati yake,[p]
kama ninavyoishi,' asema
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova, 'hawangekomboa wana
wala mabinti, bali wao, wao we-
nyewe tu, ndio wangekombole-
wa.'"[q]
19 "'Au kama ningeileta ta-
uni juu ya nchi hiyo[r] nami ni-
mwage ghadhabu yangu juu
yake pamoja na damu,[s] ili ku-

SURA 14

a Ezr 9:6
b Law 26:26
c Isa 3:1
Yer 15:2
d Yer 7:20
e Mwa 6:8
Isa 54:9
Ebr 11:7
f Da 10:11
g Ayu 1:8
Ayu 42:8
h Met 11:4
Yer 15:1
i 2Pe 2:9
j 2Fa 17:25
k Law 26:22
2Fa 2:24
l Yer 15:3
m Mwa 19:29
Ebr 11:7
n Law 26:25
Yer 25:9
Eze 5:12
Eze 21:3
Eze 38:21
o Yer 33:12
Eze 25:13
Ho 4:3
Sef 1:3
p Eze 14:14
q 1Pe 1:17
2Pe 2:9
Ufu 20:13
r Kum 28:21
2Sa 24:15
Yer 14:12
Amo 4:10
s Eze 7:8
Eze 36:18

Safu ya 2

a Mwa 7:1
b Eze 28:3
c Ayu 1:8
Ayu 42:8
d Eze 14:14
e Eze 18:20
Ho 10:12
Sef 2:3
f Yer 15:2
g Eze 5:17
Eze 33:27
h Yer 32:43
i Kum 4:31
2Nya 36:20
Isa 6:13
Isa 10:20
Eze 6:8
Mik 5:7
j Yer 3:25
Eze 6:9
Eze 20:43
k Mwa 18:20
Ne 9:33
Yer 22:9
Eze 8:6
Eze 9:9
Da 9:7
Ro 2:5

SURA 15

l Kum 32:32
Zb 80:8
Isa 5:1
Mk 12:1

mkatilia mbali mtu wa udo-
ngo na mnyama wa kufugwa,
20 hata kama Noa,[a] Danieli[b]
na Ayubu[c] wangekuwa kati-
kati yake,[d] kama ninavyoishi,'
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova, 'hawangekomboa
mwana wala binti; wao wenye-
we kwa sababu ya uadilifu wao
wangeikomboa nafsi yao.'"[e]
21 "Kwa maana hivi ndivyo
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova amesema, 'Hivyo, pia,
ndivyo itakavyokuwa waka-
ti kutakapokuwa na huku-
mu zangu nne zenye madha-
ra[f]—upanga na njaa na mnya-
ma-mwitu mwenye kudhuru
na tauni[g]—nitakazoleta juu
ya Yerusalemu ili kumkatilia
mbali kutoka humo mtu wa
udongo na mnyama wa kufu-
gwa.[h] **22** Lakini, tazama! ja-
mii iliyoponyoka hakika itaba-
ki ndani yake, wale wanaole-
twa.[i] Wana na mabinti, taza-
ma! Wanawatokea ninyi, nanyi
mtalazimika kuona njia yao
na shughuli zao.[j] Nanyi ha-
kika mtafarijiwa juu ya msi-
ba ambao nitakuwa nimeuleta
juu ya Yerusalemu, naam, yote
nitakayokuwa nimeleta juu
yake.'"
23 "'Na hakika wao wata-
wafariji ninyi wakati ambapo
mtaiona njia yao na shughuli
zao; nanyi mtalazimika kujua
kwamba sitakuwa nimetenda,
bila sababu, yote hayo amba-
yo lazima nitatenda juu yake,'
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova."[k]

15 Nalo neno la Yehova li-
kaendelea kunijia, na
kusema: **2** "Mwana wa bina-
damu, mzabibu[l] hutofautiana-
je na kila mti mwingine, hilo

chipukizi, ambalo limekuja
kuwa kati ya miti ya msituni? **3** Je, ufito huchukuliwa
kutoka kwa huo ili kuutumia
kufanyia kazi? Au watu hu-
chukua kutoka kwa huo kijiti ili kuning'iniza aina yoyote ya chombo juu yake? **4** Tazama! Lazima utiwe motoni
uwe kuni.[a] Hakika moto hute-
keteza miisho yake yote miwili, na sehemu yake ya katikati
huungua.[b] Je, unafaa kwa kazi
yoyote? **5** Tazama! Unapo-
kuwa mzima, hautumiwi kwa
kazi yoyote. Itakuwaje basi wakati ambapo moto umeuteke-
teza nao umeungua, je, kwa
kweli unaweza kutumiwa tena
kwa kazi zaidi!"[c]

6 "Kwa hiyo hivi ndivyo
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova amesema, 'Kama vile
mzabibu kati ya miti ya msituni, ambao nimeupa moto uwe
kuni, ndivyo nimewatoa waka-
aji wa Yerusalemu.[d] **7** Nami
nimeukaza uso wangu juu yao.[e]
Wametoka motoni, lakini moto
wenyewe utawateketeza.[f] Na-
nyi mtalazimika kujua kwa-
mba mimi ni Yehova, nitakapo-
uelekeza uso wangu juu yao.'"[g]

8 "'Nami nitaifanya nchi
iwe mahame yenye ukiwa,[h]
kwa sababu wametenda kwa
kukosa uaminifu,'[i] asema Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova."

16 Nalo neno la Yehova li-
kazidi kunijia, na kuse-
ma: **2** "Mwana wa binadamu,
julisha[j] Yerusalemu machu-
kizo yake.[k] **3** Nawe utasema,
'Hivi ndivyo Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova ameambia
Yerusalemu: "Asili yako na ku-
zaliwa kwako ni katika nchi ya
Mkanaani.[a] Baba yako aliku-
wa Mwamori,[b] na mama yako
alikuwa Mhiti.[c] **4** Na kuhusu
kuzaliwa kwako, katika siku
ya kuzaliwa[d] kwako uzi wa
kitovu chako haukuwa ume-
katwa, na katika maji huku-
wa umeoshwa ili usafishwe,
nawe hukuwa kamwe umepa-
kwa chumvi, wala hukuwa
umefungwa kwa nguo kamwe.
5 Hakuna jicho lililokusikitik-
ika ili kukufanyia moja la ma-
mbo haya kwa kukuhurumia,[e]
bali ulitupwa kwenye uso wa
uwanja kwa sababu nafsi yako
ilichukiwa katika siku ya kuza-
liwa kwako.

6 "'"Nami nilipita kando
yako na kukuona ukitupatu-
pa mateke katika damu yako,
nami nikakuambia katika damu
yako, 'Endelea kuishi!'[f] naam,
kukuambia wewe katika damu
yako, 'Endelea kuishi!' **7** Ni-
likufanya uwe umati mkubwa
sana kama kuchipuka kwa
shamba ili uwe mkubwa[g] na
kuwa mkuu na kuingia ndani
ukiwa na pambo bora kabisa.[h]
Yale maziwa mawili yalikomaa
kabisa, nywele zako mwenye-
we zikakua sana, ulipokuwa
uchi na tupu."'

8 "'Nami nikaja nikipita ka-
ndo yako nikakuona, na, taza-
ma! wakati wako ulikuwa wa-
kati wa maonyesho ya upendo.[i]
Kwa hiyo nikatandaza upi-
ndo wa nguo yangu juu yako[j]
na kuufunika utupu wako na
kukutolea ahadi yenye kiapo
na kuingia katika agano pamo-
ja nawe,'[k] asema Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova, 'na kwa
hiyo ukawa wangu.[l] **9** Tena,
nikakuosha kwa maji[m] na ku-
iosha damu yako kutoka juu

SURA 15
a Zb 80:16
Yoh 15:6
b Isa 1:31
Amo 4:11
c Mal 4:1
d Isa 5:24
Yer 4:7
Yer 7:20
Eze 20:47
e Law 17:10
Zb 34:16
Eze 14:8
f Amo 5:19
g Kut 14:4
Zb 9:16
Eze 6:7
Eze 7:4
h Isa 6:11
Yer 25:11
Eze 6:14
i 2Nya 36:14

SURA 16
j Isa 58:1
Eze 20:4
Eze 22:2
Eze 23:36
k Eze 8:10

Safu ya 2
a Yos 10:5
1Nya 1:13
1Nya 1:14
b 1Fa 21:26
2Fa 21:11
Eze 16:45
c Mwa 10:15
d Ho 2:3
e Isa 49:15
f Zb 147:20
Ro 9:15
g Mwa 22:17
Kut 1:7
Kut 12:37
Kum 1:10
Mdo 7:17
h Kum 4:8
Ne 9:22
i Kum 7:8
j Ru 3:9
1Sa 12:22
Isa 41:9
k Kut 19:5
Kum 4:31
Yer 2:2
l Kum 26:18
Kum 32:9
m Zb 26:6
Isa 1:16

yako na kukupaka mafuta.[a]
10 Nami nikakuvika vazi lililopambwa[b] na kukuvika viatu
vya ngozi ya sili[c] na kukufunika kwa kitani bora[d] na kukufunika kwa kitambaa cha bei.
11 Nami nikakupamba kwa mapambo na kuweka vikuku[e]
juu ya mikono yako na mkufu[f] shingoni mwako. **12** Tena, nikaweka pete ya puani[g] katika pua yako na vipuli katika masikio[h] yako na taji zuri kichwani pako.[i] **13** Nawe ukaendelea kujipamba kwa dhahabu na fedha, nayo mavazi yako yalikuwa kitani bora na kitambaa cha bei na vazi lililopambwa.[j] Chakula chako kilikuwa unga laini na asali na mafuta,[k] nawe ukawa mrembo, mrembo sana, na mwishowe ukastahili kwa ajili ya cheo cha kifalme.'"[l]

14 "'Nalo jina lako likaanza kuenea kati ya mataifa kwa sababu ya urembo wako, kwa maana ulikuwa kamili kwa sababu ya fahari yangu niliyoiweka juu yako,'[m] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

15 "'Lakini ulianza kuutegemea urembo wako[n] nawe ukawa kahaba kwa sababu ya jina lako[o] na kumimina matendo yako ya ukahaba kwa kila mpita-njia;[p] ukawa wake.
16 Nawe ukachukua sehemu ya mavazi yako na kujifanyia mwenyewe mahali pa juu[q] penye rangi mbalimbali nawe ukawa ukifanya ukahaba juu yake[r]—mambo hayo hayaingii, na hayapasi kutukia hivyo.
17 Nawe ukawa ukichukua vyombo vyako vyenye kupendeza kutoka katika dhahabu

SURA 16

a Zb 23:5
b Kut 28:6
Isa 62:3
c Kut 25:5
Kut 26:14
d Kut 39:27
e Mwa 24:22
Isa 3:19
f Wim 4:9
g Mwa 24:47
Isa 3:21
h Kut 35:22
i Kut 28:36
j Zb 48:2
k Kum 7:13
Yer 41:8
l Kum 32:13
2Sa 5:3
1Fa 4:21
m Kum 4:6
2Sa 7:23
1Fa 10:1
Zb 50:2
Omb 2:15
n Kum 32:15
Yer 7:4
Mik 3:11
Sef 3:11
o 1Fa 11:5
Zb 106:35
Isa 1:21
Isa 57:8
Yer 2:20
Ho 1:2
Yak 4:4
p Yer 3:13
q 1Fa 14:23
2Nya 21:11
r 2Fa 23:7
Eze 7:20

Safu ya 2

a Kut 32:2
Yer 10:4
b Isa 57:8
Eze 16:26
Eze 23:20
c Yer 3:9
d Eze 8:11
Eze 23:41
e Kum 32:13
Ho 2:8
f 2Fa 22:17
Yer 7:9
g Kut 13:2
Zb 106:38
h 2Fa 16:3
2Nya 33:6
Isa 57:5
Yer 7:31
Yer 32:35
Eze 20:26
i Zb 106:37
Yer 2:34
j Law 18:21
Law 20:2
2Fa 17:17
2Fa 23:10
k Yer 2:2
Ho 2:3
Ho 11:1
l Yer 13:27
Sef 3:1
m Law 26:30
Zb 78:58
Isa 57:5
Yer 2:20
Yer 3:2
n Met 9:14
o Yer 6:15
p Yer 2:24
Eze 23:9
q Eze 23:30

yangu na katika fedha yangu niliyokuwa nimekupa wewe[a] nawe ukawa ukijifanyia mwenyewe sanamu za mwanamume[b] na kufanya ukahaba nazo.[c]
18 Nawe ukawa ukiyachukua mavazi yako yaliyopambwa na kuzifunika; na mafuta yangu na uvumba[d] wangu ukawa ukiweka mbele yake. **19** Na mkate wangu niliokuwa nimekupa wewe—unga laini na mafuta na asali nilivyokuwa nimekulisha[e]—uliviweka viwe harufu yenye kutuliza[f] mbele yake, na ikaendelea kutukia hivyo,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

20 "'Nawe ulikuwa ukiwachukua wana na binti zako uliokuwa umenizalia,[g] na ukawa ukiwatoa dhabihu kwao ili wamezwe[h]—je, matendo yako hayo ya ukahaba hayatoshi?
21 Nawe ukawa ukiwachinja wanangu,[i] na kwa kuwafanya wapite katikati ya moto ukawa ukiwatolea hao.[j] **22** Na katika machukizo yako yote na matendo yako ya ukahaba hukukumbuka siku za ujana wako ulipokuwa uchi na tupu; ulikuwa ukitupatupa mateke katika damu yako.[k] **23** Kwa hiyo ikawa kwamba baada ya ubaya wako wote ("ole, ole wako,"[l] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova) **24** ulijijengea kilima na kujifanyia kilele katika kila kiwanja cha watu wote.[m] **25** Katika kila kichwa cha njia ulikijenga kilele[n] chako nawe ukaanza kuufanya urembo wako kuwa chukizo[o] na kumpanulia miguu yako kila mpita-njia[p] na kuzidisha matendo yako ya ukahaba.[q]
26 Nawe ukafanya ukahaba

na wana wa Misri,[a] jirani zako
wenye kiungo kikubwa,[b] nawe
ukaendelea kuufanya ukaha-
ba wako uwe mwingi ili kuni-
tia uchungu. **27** Na, tazama!
hakika nitaunyoosha mkono
wangu juu yako[c] nami nitapu-
nguza posho lako[d] na kukutia
katika tamaa ya nafsi[e] ya wa-
nawake wanaokuchukia,[f] binti
za Wafilisti,[g] wanawake wali-
ofedheheshwa kwa sababu ya
njia yako kuhusiana na mwe-
nendo mpotovu.[h]

28 "'Nawe ukaendelea kufa-
nya ukahaba na wana wa Ashu-
ru kwa sababu hukutoshele-
zwa,[i] nawe ukaendelea kufa-
nya ukahaba pamoja nao, nawe
hukutoshelezwa pia. **29** Kwa
hiyo ukazidi kuufanya ukaha-
ba wako uwe mwingi kuele-
kea nchi ya Kanaani,[j] kuwaele-
kea Wakaldayo;[k] na hata katika
hilo hukutoshelezwa. **30** Lo!
Jinsi nilivyojaa ghadhabu[l] juu
yako,' asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova, 'kwa kufa-
nya kwako mambo yote haya,
kazi ya mwanamke,[m] kahaba
mwenye kutawala![n] **31** Uli-
pojenga kilima chako kwenye
kichwa cha kila njia na ku-
fanya kilele chako mwenye-
we katika kila kiwanja cha
watu wote, hata hivyo uka-
wa tofauti na kahaba kwa ku-
dharau malipo. **32** Kuhusu
mwanamke anayefanya uzinzi,
yeye huwachukua wageni ba-
dala ya mume wake mwenye-
we.[o] **33** Watu wana destu-
ri ya kuwapa zawadi makaha-
ba wote,[p] lakini wewe—wewe
umewapa zawadi wote wanao-
kupenda kwa tamaa,[q] nawe
unawapa rushwa waingie kwa-
ko kutoka pande zote katika

SURA 16

a 2Fa 23:34
Isa 30:2
Isa 30:3
Yer 2:36
Omb 5:6
Eze 20:7
b Isa 57:8
Eze 23:20
c Isa 5:25
d Kum 28:48
e Isa 56:11
f Zb 106:41
g 2Nya 28:18
h Yer 2:11
Eze 5:6
i 2Fa 16:7
2Nya 28:23
Yer 2:18
Eze 23:5
j Amu 2:12
2Fa 21:9
k Eze 23:14
l Kum 29:28
m Yer 3:3
n Met 7:11
o Yer 2:25
Yer 3:1
Yer 3:20
Ho 3:1
p Mwa 38:16
Kum 23:18
Ho 2:12
Lu 15:30
q Isa 57:9
Ho 8:9

Safu ya 2

a 2Nya 16:2
b Isa 1:21
Yer 3:6
Ho 2:5
c Eze 13:2
d Omb 1:9
e Eze 16:37
f Eze 23:9
Ho 2:5
g 1Fa 15:12
2Fa 17:12
2Fa 21:11
h Zb 106:38
Yer 2:34
i Yer 13:22
Omb 1:8
Ho 2:10
Nah 3:5
j Mwa 38:24
Law 20:10
Kum 22:22
k Mwa 9:6
Kut 21:12
Zb 79:3
l Eze 23:25
Nah 1:2
Sef 1:17
m Eze 16:24
n Isa 27:9
o Isa 3:18
Yer 4:30
Eze 23:26
Ho 2:3
p Isa 3:20

matendo[a] yako ya ukahaba.
34 Na kukuhusu wewe jambo
lililo kinyume linatukia tofa-
uti na walivyo wanawake we-
ngine katika matendo yako ya
ukahaba, na hakuna ukahaba
ambao umefanywa kama wa
mtindo wako, naam, kwa wewe
kutoa malipo wakati ambapo
hakuna malipo uliyopewa, na
kwa hiyo mambo yanatukia ki-
nyume.'

35 "Kwa hiyo, Ee kahaba,[b] li-
sikie neno la Yehova.[c] **36** Hivi
ndivyo Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema, 'Kwa sa-
babu uchu wako umemiminwa[d]
nazo sehemu zako za siri[e] zime-
funuliwa katika matendo yako
ya ukahaba kuwaelekea wale
wanaokupenda[f] kwa tamaa na
kuelekea sanamu zako zote za
mavi zenye kuchukiza,[g] hata
kwa damu ya wana wako ambao
ulizipa hizo,[h] **37** kwa hiyo, ta-
zama, ninawakusanya pamoja
wote wanaokupenda kwa tamaa
ambao ulikuwa mwenye kupe-
ndeza kwao na wale wote ulio-
wapenda pamoja na wale wote
uliowachukia, nami nitawaku-
sanya hao pamoja juu yako ku-
toka pande zote na kuwafunulia
sehemu zako za siri, nao watazi-
ona sehemu zako zote za siri.[i]

38 "'Nami nitakuhukumu
kwa hukumu za wanawake wa-
zinzi[j] na wanawake wanao-
mwaga damu,[k] nami nitakupa
damu ya ghadhabu na wivu.[l]
39 Nami nitakutia mkononi
mwao, nao hakika watakibo-
moa kilima[m] chako na vilele
vyako hakika vitabomolewa,[n]
nao watakuvua mavazi[o] yako
na kuvichukua vyombo vyako
vyenye urembo[p] na kukuacha
ukiwa uchi na tupu. **40** Nao

wataleta kutaniko[a] juu yako
na kukupiga kwa mawe[b] na
kukuchinja kwa panga zao.[c]
41 Nao wataziteketeza nyu-
mba zako kwa moto[d] na ku-
fanya ndani yako matendo ya
hukumu mbele ya macho ya
wanawake wengi;[e] nami nita-
kufanya uache kuwa kahaba,[f]
na pia hutatoa malipo yoyo-
te tena. **42** Na ghadhabu ya-
ngu nitaituliza ndani yako,[g]
na wivu wangu utageukia
mbali nawe;[h] nami nitakaa ki-
mya wala sitaendelea kuwa na
uchungu tena.'

43 "'Kwa sababu hukuziku-
mbuka siku za ujana wako[i]
nawe ulikuwa ukinisumbua
kwa sababu ya mambo yote
haya,[j] hata hapa mimi pia, nita-
iweka njia yako mwenyewe juu
ya kichwa chako mwenyewe,'[k]
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova, 'nawe hakika hu-
taendeleza mwenendo mpoto-
vu wowote pamoja na machu-
kizo yako yote.

44 "'Tazama! Kila mtu ana-
yetumia methali[l] juu yako ata-
itumia methali, na kusema:
"Kama mama ndivyo binti ali-
vyo!"[m] **45** Wewe ni binti ya
mama yako,[n] anayemchukia
mume[o] wake na wanawe. Na
wewe ni dada ya dada zako,
waliowachukia waume zao
na wana wao. Mama yenu ni-
nyi wanawake alikuwa Mhiti,[p]
na baba yenu alikuwa Mwa-
mori.'"[q]

46 "'Na dada yako mkubwa
ni Samaria[r] pamoja na miji
yake ya kandokando,[s] anaye-
kaa upande wako wa kusho-
to, na dada yako aliye mdogo
wako, anayekaa upande wako
wa kuume, ni Sodoma[t] pamoja
na miji yake ya kandokando.[a]
47 Nawe hukutembea katika
njia zao, wala hukufanya kuli-
ngana na machukizo yao.[b] Ba-
ada ya kitambo kidogo sana
hata ulianza kutenda kwa uha-
ribifu zaidi kuliko walivyo-
fanya katika njia zako zote.[c]
48 Kama ninavyoishi,' asema
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova, 'Sodoma dada yako, yeye
pamoja na miji yake ya kando-
kando, hajatenda kulingana na
uliyotenda, wewe na miji yako
ya kandokando.[d] **49** Tazama!
Hili ndilo lililokuwa kosa la
Sodoma dada yako: Yeye pa-
moja na miji yake ya kandoka-
ndo[e] walikuwa na kiburi,[f] uto-
shelevu wa mkate[g] na ukose-
fu wa wasiwasi[h] wa kukaa bila
usumbufu, naye hakuutia ngu-
vu mkono wa mwenye kutese-
ka na aliye maskini.[i] **50** Nao
wakaendelea kuwa wenye ma-
jivuno[j] na kuendeleza chuki-
zo mbele zangu,[k] na mwishowe
mimi nikawaondoa, kama nili-
vyoona kuwa inafaa.[l]

51 "'Naye Samaria,[m] hajaten-
da dhambi hata kufikia nusu
ya dhambi zako, lakini wewe
uliendelea kuyafanya machu-
kizo yako yawe mengi kuliko walivyotenda, hivi kwamba
ukawafanya dada zako waone-
kane kuwa waadilifu kwa sa-
babu ya machukizo yako yote
uliyoyaendeleza.[n] **52** Wewe
pia, beba fedheha yako uta-
kapolazimika kuwatetea dada
zako. Kwa sababu ya dhambi
zako ambazo ulitenda kwa njia
yenye kuchukiza zaidi kuliko walivyotenda, wao ni wa-
adilifu zaidi kuliko wewe.[o] Na
wewe pia, na upate aibu na ku-
beba fedheha yako kwa kuwa

SURA 16

a Eze 23:46
Hab 1:6
b Kum 22:21
c 2Nya 36:17
Yer 25:9
d Law 26:33
2Fa 25:9
Yer 39:8
e Eze 5:8
f Eze 23:27
g Eze 5:13
h Isa 40:2
i Zb 78:42
Yer 2:32
j Zb 95:10
k Eze 9:10
Eze 11:21
Eze 22:31
l 1Sa 24:13
Eze 18:2
m 1Fa 21:26
2Fa 21:9
Ezr 9:1
Zb 106:35
n Eze 16:3
o Isa 1:4
Isa 54:5
Ho 2:2
p Eze 16:3
q Kum 9:5
Kum 20:17
Yos 10:5
2Fa 21:11
r Eze 23:33
s Yer 3:8
t Mwa 18:20
Mwa 19:24
Kum 29:23
Kum 32:32
Isa 1:10
Isa 3:9
Yer 23:14
Yud 7

Safu ya 2

a Mwa 19:25
b 1Fa 16:31
c 2Fa 21:9
Eze 5:6
d Mt 10:15
Mt 11:24
e Yud 7
f Mwa 19:9
Met 16:5
Met 16:18
Met 21:4
Yak 4:16
g Mwa 13:10
Kum 8:10
Kum 32:15
Met 30:9
Lu 12:21
h Met 1:32
i Met 21:13
Eze 18:12
j Met 16:18
Isa 3:16
Yer 13:15
1Pe 5:5
k Mwa 13:13
Mwa 18:20
Mwa 19:5
l Mwa 19:24
Isa 13:19
Yer 49:18
Omb 4:6
2Pe 2:6
m 2Fa 21:13
Yer 23:13
Eze 23:33
n Yer 3:11
Mt 12:41
o 1Fa 2:32

unawafanya dada zako waonekane kuwa waadilifu.'

53 "'Nami nitawakusanya mateka wao,[a] mateka wa Sodoma na wa miji yake ya kandokando, na mateka wa Samaria na wa miji yake ya kandokando; pia nitawakusanya mateka wako katikati yao,[b] **54** ili uibebe fedheha yako;[c] nawe utafedheheka kwa sababu ya yote ambayo umefanya, kwa kuwa uliwafariji.[d] **55** Na dada zako wenyewe, Sodoma na miji yake ya kandokando, watarudi kwenye hali yao ya kwanza, na Samaria na miji yake ya kandokando watarudi kwenye hali yao ya kwanza, na wewe mwenyewe na miji yako ya kandokando mtarudi kwenye hali yenu ya kwanza.[e] **56** Na Sodoma dada yako hakuwa kitu kinachostahili kusikiwa kutoka kinywani mwako katika siku ya fahari yako,[f] **57** kabla ubaya wako mwenyewe haujafunuliwa,[g] kama katika ule wakati wa shutuma ya binti za Siria[h] na za wote waliomzunguka pande zote, binti za Wafilisti,[i] wale wanaokutendea kwa dharau pande zote.[j] **58** Mwenendo wako mpotovu[k] na machukizo yako, wewe mwenyewe lazima uyabebe,'[l] asema Yehova."

59 "Kwa maana hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema, 'Mimi pia lazima nikutendee wewe kama vile ulivyotenda,[m] kwa sababu ulikidharau kiapo kwa kuvunja agano langu.[n] **60** Nami, mimi mwenyewe, nitalikumbuka agano langu pamoja nawe katika siku za ujana wako,[o] nami nitakufanyia wewe agano lenye kudumu mpaka wakati usio na kipimo.[a] **61** Nawe hakika utazikumbuka njia zako[b] na kufedheheka unapowapokea dada zako, walio wakubwa wako na walio wadogo wako, nami hakika nitakupa wao wawe mabinti,[c] lakini si kwa sababu ya agano lako.'[d]

62 "'Na mimi, mimi mwenyewe, nitalifanya agano langu pamoja nawe;[e] nawe utalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova, **63** ili ukumbuke na kuona aibu[f] nawe usije kamwe kuwa na sababu ya kufungua kinywa[g] chako kwa sababu ya kufedheheka kwako, nitakapofanya upatanisho[h] kwa ajili yako kwa sababu ya yote ambayo umetenda,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

17 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** "Mwana wa binadamu, tega kitendawili[i] na utunge neno la kimethali kuelekea nyumba ya Israeli.[j] **3** Nawe utasema, 'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: "Tai mkubwa,[k] mwenye mabawa makubwa,[l] na manyoya marefu, aliyejaa manyoya, yaliyokuwa na rangi mbalimbali, alikuja Lebanoni[m] na kukichukua kilele[n] cha mwerezi.[o] **4** Aliking'oa kilele cha machipukizi yake machanga, akakileta mpaka nchi ya Kanaani;[p] akakiweka katika jiji la wafanya-biashara. **5** Tena, akachukua sehemu ya mbegu ya nchi[q] hiyo na kuiweka katika shamba la mbegu. Akaiweka kama mvinje kando ya

SURA 16

a Zb 14:7
Zb 126:1
Isa 1:9
b Isa 19:24
c Yer 2:26
Eze 36:31
d Eze 14:22
e Eze 36:11
Mal 3:4
f Isa 65:5
Sef 3:11
g Omb 4:22
Eze 21:24
Ho 2:10
h 2Fa 16:5
2Nya 28:5
Isa 7:1
i 2Nya 28:18
j Yer 33:24
k Ga 5:19
1Pe 4:3
l Omb 5:7
Eze 23:49
m Zb 62:12
Isa 3:11
Ro 2:6
Ga 6:7
n Kum 29:12
Yer 22:9
o Law 26:42
Zb 106:45

Safu ya 2

a Yer 32:40
Yer 50:5
b Eze 20:43
c Isa 54:1
Ga 4:26
d Yer 31:31
Ebr 8:13
e Ho 2:19
f Ezr 9:6
Eze 36:31
g Zb 39:9
Ro 3:19
h Zb 103:12
Mik 7:19

SURA 17

i Amu 14:12
Met 1:6
j Eze 20:49
Ho 12:10
Mt 13:13
k Kum 28:49
Yer 4:13
Omb 4:19
Ho 8:1
l Da 7:4
m Yer 22:23
n Yer 22:7
o 2Fa 24:12
2Nya 36:10
Yer 24:1
p 2Fa 24:15
q Yer 37:1
Eze 17:13

maji mengi,[a] kama mti wa mvinje. **6** Nayo ikaanza kuchipuka na hatua kwa hatua ikawa mzabibu wenye majani mengi na ulio mfupi,[b] wenye mwelekeo wa kugeuza majani yake kuelekea ndani; nayo mizizi yake, hatua kwa hatua ikaja kuwa chini yake. Nao mwishowe ukawa mzabibu, ukazaa machipukizi na kutokeza matawi.[c]

7 "'"Na kukawa na tai mwingine mkubwa,[d] mwenye mabawa makubwa, na mwenye manyoya makubwa,[e] na, tazama! mzabibu huohuo ukasambaza mizizi yake kwa pupa kumwelekea.[f] Nao ukamnyooshea majani yake ili ayanyweshe, mbali na eneo dogo la bustani mahali ulipopandwa.[g] **8** Katika shamba zuri, kando ya maji mengi, tayari ulikuwa umepandikizwa,[h] ili utokeze matawi na kuzaa matunda, uwe mzabibu mkubwa."'

9 "Sema, 'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: "Je, huo utakuwa na mafanikio?[i] Je, mtu fulani hataing'oa mizizi yake[j] na kuyafanya matunda yake yawe na magamba? Na je, machipukizi yake yote yaliyokatwa hivi karibuni hayatakauka?[k] Utakauka. Hautainuliwa kutoka mizizini mwake kwa mkono wenye nguvu wala kwa umati wa watu. **10** Na, tazama! ijapokuwa ulipandikizwa, je, utakuwa na mafanikio? Je, hautakauka kabisa, kama wakati ambapo upepo wa mashariki huugusa?[l] Utakauka katika eneo dogo la bustani la chipukizi lake."'"[m]

11 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **12** "Iambie, tafadhali, nyumba yenye kuasi,[a] 'Je, ninyi kwa kweli hamjui maana ya mambo haya?' Sema, 'Tazama! Mfalme wa Babiloni alikuja Yerusalemu, akamchukua mfalme wake[b] na wakuu wake na kuwaleta Babiloni kwa ajili yake.[c] **13** Tena, alichukua mmoja wa uzao wa kifalme,[d] akafanya agano naye na kumwingiza katika kiapo;[e] na watu wa kwanza kabisa wa nchi akawachukua,[f] **14** ili ufalme huo ushuke,[g] usiweze kujiinua, ili kwa kushika agano lake uweze kusimama.[h] **15** Lakini mwishowe alimwasi[i] kwa kutuma wajumbe wake Misri, ili wampe farasi[j] na umati wa watu. Je, atakuwa na mafanikio? Je, ataponyoka, yeye anayefanya mambo haya, na ambaye amevunja agano? Na je, kwa kweli ataponyoka?'[k]

16 "'"Kama ninavyoishi,"[l] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, "mahali pa mfalme aliyemweka kuwa mfalme yule aliyekidharau kiapo[m] chake na ambaye alilivunja agano lake, atakufa pamoja naye katikati ya Babiloni.[n] **17** Na kwa jeshi kubwa na kwa kutaniko lenye watu wengi Farao hatamfanya apate mafanikio katika vita,[o] kwa kujenga boma la kuzingira na kwa kujenga ukuta wa kuzingira, ili kukatilia mbali nafsi nyingi.[p] **18** Naye amedharau kiapo kwa kuvunja agano,[q] na, tazama! alikuwa ameutia mkono[r] wake naye amefanya mambo yote hayo. Yeye hataponyoka."'[s]

SURA 17

a 2Fa 24:17
b Eze 17:14
c 2Nya 36:11
d Yer 37:5
Eze 17:15
e Yer 37:7
f Isa 36:6
g 2Fa 24:20
2Nya 36:13
h Yer 37:1
i Hes 14:41
2Nya 13:12
Yer 32:5
j Yer 21:7
k 2Fa 25:7
Yer 52:10
l Ho 13:15
Yon 4:8
m Eze 19:12

Safu ya 2

a Isa 1:2
Eze 2:5
Eze 3:9
Eze 12:9
b 2Fa 24:12
Yer 22:25
c Isa 39:7
Yer 52:32
d 2Fa 24:17
Yer 37:1
e 2Nya 36:13
Yer 5:2
f 2Fa 24:15
Yer 24:1
g Kum 28:43
1Sa 2:7
h Yer 27:12
Yer 38:17
i 2Fa 24:20
2Nya 36:13
Yer 52:3
Eze 17:7
j Kum 17:16
Isa 30:2
Isa 31:1
Yer 37:5
k Met 19:5
Yer 32:4
l Ebr 6:13
m Mal 3:5
n Yer 34:3
Yer 52:11
o Isa 31:1
Yer 37:7
Omb 4:17
Eze 29:6
p Yer 33:5
q Mt 5:37
Ro 1:31
r Omb 5:6
s Eze 17:15

19 "'Kwa hiyo, hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: "Kama ninavyoishi, hakika kiapo changu ambacho amekidharau[a] na agano langu ambalo amelivunja—nitamletea juu ya kichwa chake. **20** Nami nitautandaza wavu wangu juu yake, naye hakika atakamatwa katika wavu wangu wa kuwindia;[b] nami nitamleta Babiloni na kujiweka katika hukumu pamoja naye huko kuhusiana na ukosefu wake wa uaminifu alionitendea.[c] **21** Nao wakimbizi wake wote katika vikosi vyake vyote, wataanguka kwa upanga, nao wanaobaki watatawanywa kotekote kuelekea kila upepo.[d] Nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimesema hilo."'[e]

22 "'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: "Mimi mwenyewe nitachukua pia na kuweka sehemu ya vilele vilivyo juu sana vya mierezi;[f] kutoka juu ya vitawi vyake nitang'oa kitawi kichanga[g] nami mwenyewe nitakipandikiza juu ya mlima mrefu na ulio juu sana.[h] **23** Kwenye mlima wa kilele cha Israeli nitakipandikiza,[i] nacho hakika kitazaa matawi na kutokeza matunda[j] na kuwa mwerezi mkubwa.[k] Na chini yake hakika watakaa ndege wote wenye mabawa ya kila aina; watakaa katika uvuli wa majani yake.[l] **24** Na miti yote ya shambani italazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova,[m] nimeushusha ule mti mrefu,[n] nimeuweka juu ule mti mfupi,[o] nimeukausha ule mti ambao ungali mbichi[a] na kuufanya mti uliokauka uchipuke. Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema nami nimefanya[b] hilo."'"

18 Na neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** "Inamaanisha nini kwenu kwamba mnataja neno hili la kimethali kwenye udongo wa Israeli, na kusema, 'Akina baba ndio wanaokula zabibu mbichi, lakini meno ya wana ndiyo yanayotiwa ukakasi'?[c]

3 "'Kama ninavyoishi,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'hamtaendelea kuwa na sababu ya kulitaja neno hili la kimethali katika Israeli. **4** Tazama! Nafsi zote—ni zangu.[d] Kama ilivyo nafsi[e] ya baba ndivyo ilivyo nafsi ya mwana—ni zangu.[f] Nafsi inayotenda dhambi[g]—hiyo yenyewe itakufa.[h]

5 "'Na mtu, ikiwa ni mwadilifu naye ametenda haki na uadilifu;[i] **6** naye hakula[j] juu ya milima[k] wala hakuyainua macho yake kuelekea sanamu za mavi za nyumba ya Israeli,[l] wala hakumnajisi mke wa mwenzake[m] wala hakumkaribia mwanamke aliye katika uchafu wake;[n] **7** wala hakumtendea vibaya mtu yeyote;[o] rehani aliyotwaa kwa ajili ya deni, alikuwa akiirudisha;[p] hakuwa akinyakua chochote kwa unyang'anyi;[q] mkate wake mwenyewe alikuwa akimpa mwenye njaa[r] na alikuwa akimvika vazi aliye uchi;[s] **8** naye hakuwa akitoa chochote apate faida[t] wala hakuwa akichukua riba yoyote;[u] naye alikuwa akiuepusha mkono wake na ukosefu wa

SURA 17
a Kum 5:11
Yer 5:2
b 2Nya 33:11
Eze 12:13
Eze 32:3
Ho 7:12
c Eze 20:36
Mik 6:2
d Eze 5:10
Eze 12:14
e Eze 6:13
f Zb 80:15
Isa 11:1
Yer 23:5
Yer 33:15
Zek 3:8
g Isa 53:2
h Zb 2:6
i Zb 92:13
Da 4:17
j Isa 27:6
k Zb 92:12
l Zb 72:8
Ho 14:7
m Isa 55:12
n 1Sa 2:7
Zb 75:7
Lu 1:52
o Isa 9:6
Eze 21:27
Da 4:17
Amo 9:11

Safu ya 2
a Lu 23:31
b Eze 22:14
Eze 24:14

SURA 18
c Yer 15:4
Yer 31:29
Omb 5:7
d Zb 100:3
Mdo 17:26
e Mwa 2:7
f Kum 26:18
g Ro 3:23
Ro 5:12
h Mwa 2:17
Mwa 17:14
Amu 16:30
Ayu 33:22
Zb 78:50
Isa 53:12
Mdo 3:23
Ro 6:23
Ufu 16:3
i Zb 15:2
j Hes 25:2
Eze 22:9
k Kum 12:2
Yer 3:6
Ho 4:13
l Eze 36:25
m Law 20:10
n Law 18:19
Law 20:18
o Law 25:14
Met 14:21
p Kum 24:12
Eze 33:15
q Law 6:2
r Kum 15:11
Met 28:27
s Isa 58:7
Mt 25:36
Yak 2:15
t Kut 22:25
Kum 23:19
Zb 15:5
Lu 6:35
u Law 25:36
Ne 5:7

haki;[a] naye alikuwa akiitenda
haki ya kweli kati ya mtu na
mwenzake;[b] **9** naye aliendelea kutembea katika amri zangu[c] na aliyashika maamuzi
yangu ya hukumu ili kutenda
kweli,[d] yeye ni mwadilifu.[e] Hakika yeye ataendelea kuishi,'[f]
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova.

10 "'Na ikiwa mtu amemzaa
mwana ambaye ni mnyang'anyi,[g] mmwagaji wa damu,[h]
ambaye amefanya jambo linalofanana na moja kati ya
mambo hayo **11** (lakini yeye
mwenyewe hajafanya lolote la
mambo hayo); ikiwa yeye pia
amekula juu ya milima,[i] naye
amemnajisi mke wa mwenzake;[j] **12** naye amemtendea vibaya mtu mwenye kuteseka
na aliye maskini;[k] naye amenyakua vitu kwa unyang'anyi,[l] naye hakuwa akirudisha
kitu kilichowekwa rehani;[m]
naye aliyainua macho yake kuelekea sanamu za mavi,[n] yeye
amefanya chukizo.[o] **13** Ametoa kwa riba,[p] na amechukua
faida,[q] naye hakika hataendelea kuishi. Ameyafanya machukizo hayo yote.[r] Hakika
atauawa. Damu yake mwenyewe itakuwa juu yake.[s]

14 "'Na, tazama! mtu amemzaa mwana, ambaye anaendelea kuona dhambi zote za
baba yake ambazo amefanya,
naye anaona lakini hafanyi
mambo kama hayo.[t] **15** Hajakula juu ya milima, naye hajayainua macho yake kuelekea sanamu za mavi za
nyumba ya Israeli;[u] hajamnajisi
mke wa mwenzake;[v] **16** wala
hajamtendea vibaya[w] mtu ye-

SURA 18

a Law 19:35
Kum 25:16
b Law 19:15
Law 25:14
Kum 1:16
Zek 8:16
c Kum 8:11
d Kum 4:1
Kum 5:1
Eze 20:11
e Zb 24:5
f Law 18:5
Ne 9:29
Amo 5:4
Ro 10:5
Ga 3:12
g Law 19:13
h Mwa 9:6
Kut 21:12
Hes 35:31
i Kut 34:15
j Law 20:10
k Kum 15:7
Ayu 31:17
Ho 12:7
l Law 6:2
m Kum 24:12
n Law 26:30
o 2Fa 21:11
p Law 25:36
Eze 22:12
q Kum 23:19
Isa 24:2
r Law 18:30
s Law 20:9
Law 20:27
Eze 3:18
Eze 33:4
Mdo 18:6
t Yer 8:6
u Law 26:30
v Law 20:10
w Kut 22:21
Met 19:26

Safu ya 2

a Kum 24:12
b Law 6:2
c Kum 15:11
Ayu 31:17
Mt 25:35
d Ayu 31:19
Isa 58:7
Yak 2:15
e Law 25:36
f Kut 22:25
Kum 23:19
g Kum 4:1
Kum 5:1
h Kum 8:11
i Eze 3:21
j Eze 18:9
k Law 19:13
l Law 6:2
m Isa 3:11
n Eze 3:18
o Kut 20:5
Kum 5:9
2Fa 23:26
p Lu 1:6
q Eze 20:18
r Kum 16:20
Eze 18:9
Ro 10:5
s Kum 24:16
2Fa 14:6
Yer 31:30
Eze 18:4
t 2Nya 25:4
u 1Fa 8:32
Isa 3:10

yote, hajachukua rehani[a] yoyote, wala hajachukua chochote
kwa unyang'anyi;[b] yeye amempa mwenye njaa mkate wake
mwenyewe,[c] na amemvika vazi
aliye uchi;[d] **17** ameuepusha
mkono wake na mwenye kuteseka; hajachukua riba[e] wala faida[f] yoyote; ameyafanya maamuzi yangu ya hukumu;[g] ametembea katika amri zangu;[h]
yeye mwenyewe hatakufa kwa
sababu ya kosa la baba yake.[i]
Hakika ataendelea kuishi.[j]
18 Naye baba yake, kwa sababu alifanya unyang'anyi[k] wa
moja kwa moja, alinyakua kitu
kwa kumnyang'anya ndugu,[l]
na lolote ambalo si zuri amelifanya katikati ya watu wake,[m]
tazama! basi lazima afe kwa ajili ya kosa lake.[n]

19 "'Nanyi hakika mtasema: "Kwa nini mwana hawezi
kuwa na hatia yoyote kwa sababu ya kosa la baba?"[o] Sasa
kwa habari ya mwana huyo,
yeye ametenda haki na uadilifu,[p] amezishika amri zangu
zote naye anaendelea kuzitenda.[q] Hakika ataendelea kuishi.[r] **20** Nafsi inayotenda
dhambi—hiyo yenyewe itakufa.[s] Mwana hatakuwa na
hatia yoyote kwa sababu ya kosa
la baba, na baba hatakuwa na hatia yoyote kwa sababu ya kosa la mwana.[t] Uadilifu wa mwadilifu utakuwa juu
yake mwenyewe,[u] nao uovu
wa mwovu utakuwa juu yake
mwenyewe.[v]

21 "'Sasa kwa habari ya mwovu, ikiwa atageuka na kuziacha dhambi zake zote ambazo
ametenda[w] naye hakika ashike

v 2Nya 6:23; Eze 33:10; Ro 2:9; Ga 6:7; w 2Nya 33:12; Isa 55:7; Eze 33:12; Mdo 3:19.

sheria zangu zote na kutenda haki na uadilifu,[a] hakika yeye ataendelea kuishi. Hatakufa.[b] **22** Makosa yake yote ambayo ametenda—hayo hayatakumbukwa juu yake.[c] Ataendelea kuishi kwa uadilifu ambao ametenda.'[d]

23 "'Je, ninapendezwa hata kidogo na kifo cha mtu mwovu,'[e] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'bali kwamba ageuke na kuziacha njia zake, naye kwa kweli aendelee kuishi?'[f]

24 "'Sasa, mtu mwadilifu anapogeuka na kuuacha uadilifu wake naye kwa kweli atende kwa njia isiyo ya haki;[g] kulingana na machukizo yote ambayo mwovu ametenda yeye anaendelea kutenda[h] naye anaishi, hakuna lolote la matendo yake ya uadilifu ambayo ametenda litakalokumbukwa.[i] Atakufa kwa sababu ya ukosefu wake wa uaminifu ambao ametenda na kwa sababu ya dhambi ambayo ametenda.[j]

25 "'Nanyi hakika mtasema: "Njia ya Yehova si sawa."[k] Sikia, tafadhali, Ee nyumba ya Israeli. Je, njia yangu mwenyewe si sawa?[l] Je, njia zenu ninyi sizo ambazo si sawa?[m]

26 "'Mtu mwadilifu anapogeuka na kuuacha uadilifu wake naye kwa kweli atende kwa njia isiyo ya haki[n] na afe kutokana nao, atakufa kwa sababu ya kutenda kwa njia isiyo ya haki.[o]

27 "'Na mwovu anapogeuka na kuuacha uovu wake ambao ameutenda naye atende haki na uadilifu,[p] yeye ndiye atakayeihifadhi hai nafsi yake mwenyewe.[a] **28** Anapoona[b] na kugeuka na kuyaacha makosa yake yote ambayo ametenda,[c] hakika yeye ataendelea kuishi. Hatakufa.[d]

29 "'Nayo nyumba ya Israeli hakika itasema: "Njia ya Yehova si sawa."[e] Nazo njia zangu, je, si sawa, Ee nyumba ya Israeli?[f] Je, njia zenu sizo ambazo si sawa?'[g]

30 "'Kwa hiyo nitawahukumu ninyi kila mmoja kulingana na njia yake,[h] Ee nyumba ya Israeli,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.[i] 'Geukeni, naam, geukeni na kuyaacha makosa yenu yote,[j] na chochote kisiwe kwenu kikwazo kinachosababisha kosa.[k] **31** Tupilieni mbali kutoka juu yenu makosa yenu yote mliyokosa[l] na kujifanyia wenyewe moyo mpya[m] na roho mpya,[n] kwa maana kwa nini mfe,[o] Ee nyumba ya Israeli?'

32 "'Kwa maana sipendezwi na kifo cha mtu anayekufa,'[p] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. 'Kwa hiyo geukeni, mwendelee kuishi.'"[q]

19 "Nawe, imba wimbo wa huzuni[r] kuhusu wakuu wa Israeli,[s] **2** nawe useme, 'Mama yako alikuwa nini? Simba-jike kati ya simba.[t] Alilala kati ya wana-simba wenye manyoya shingoni. Aliwalea watoto wake.

3 "'Na hatua kwa hatua akamlea mmoja wa watoto wake.[u] Akawa mwana-simba mwenye manyoya shingoni, naye akaanza kujifunza jinsi ya kurarua mawindo.[v] Alimrarua hata mtu wa udongo.

SURA 18

a Lu 1:6
b Eze 3:21
c 2Nya 33:13; Zb 25:7; Isa 43:25; Eze 33:16
d 2Nya 6:23
e Omb 3:33; Eze 33:11; 1Ti 2:4; 2Pe 3:9
f Mik 7:18
g 1Sa 15:11; 1Fa 11:4; Eze 33:12
h Ro 1:28
i Ebr 10:38; 2Yo 8
j Met 14:32; Met 21:16
k Ayu 34:5; Ayu 35:2; Met 19:3; Eze 33:17; Mal 2:17; Ro 9:20
l Kum 32:4; Zb 145:17
m Zb 50:21; Isa 55:9; Yer 2:17
n Kum 25:16
o Ga 6:7
p Isa 1:18; Isa 55:7; Mdo 26:20

Safu ya 2

a 1Ti 4:16
b Kum 32:29
c 1Sa 7:3; Eze 33:12
d Eze 18:9
e Zb 92:15; Met 19:3
f Mwa 18:25; Kum 32:4; Zb 145:17; Isa 40:14
g Ayu 9:2
h Ayu 34:11; Ro 2:6; 1Pe 1:17
i Mhu 12:14
j Ho 12:6; Yoe 2:13; Mt 3:2
k Ro 2:5
l Zb 34:14; Isa 1:16
m Zb 51:10; Yer 32:39
n Isa 1:19; Eze 11:19; Efe 4:24
o Kum 30:15; Met 8:36; Mdo 13:46
p Yer 29:11; Omb 3:33; Eze 33:11; Lu 15:10; 2Pe 3:9
q Kum 30:16; Eze 18:9

SURA 19

r Yer 7:29; Eze 26:17
s 2Nya 35:25
t Zb 7:2; Nah 2:11; Sef 3:3

u 2Fa 23:31; 2Nya 36:1; v 2Fa 23:32.

4 Na mataifa yakaendelea kusikia juu yake. Akakamatwa katika shimo lao, nao wakamchukua kwa kulabu mpaka katika nchi ya Misri.[a]

5 "'Mama huyo alipoona kwamba amengoja nalo tumaini lake lilikuwa limepotea, ndipo akachukua mwingine kati ya watoto wake.[b] Akamweka kuwa mwana-simba mwenye manyoya shingoni. **6** Na huyo akaanza kutembea huku na huku katikati ya simba. Akawa mwana-simba mwenye manyoya shingoni. Naye hatua kwa hatua akajifunza jinsi ya kurarua mawindo.[c] Akamrarua hata mtu wa udongo.[d] **7** Naye akaijua minara ya makao yake, akayaharibu majiji yao,[e] hivi kwamba nchi ikafanywa ukiwa naye akaijaza kwa sauti ya mngurumo wake.[f] **8** Na mataifa kuzunguka pande zote kutoka katika wilaya za utawala wakaanza kujipanga dhidi yake[g] na kuutandaza wavu wao juu yake.[h] Akakamatwa katika shimo lao.[i] **9** Mwishowe wakamweka katika tundu kwa kulabu na kumleta kwa mfalme wa Babiloni.[j] Wakamleta kwa kutumia nyavu za kuwindia, ili sauti yake isisikiwe tena katika milima ya Israeli.[k]

10 "'Mama yako[l] alikuwa kama mzabibu katika damu yako,[m] uliopandwa kando ya maji. Akawa mwenye kuzaa matunda na mwenye kujaa matawi kwa sababu ya maji mengi.[n] **11** Nayo yakawa kwake fimbo zenye nguvu, zilizokusudiwa kuwa fimbo za enzi za watawala.[o] Nacho kimo chake kikarefuka hatua kwa hatua katikati ya matawi, nao ukaonekana kwa sababu ya urefu wake, kwa sababu ya wingi wa majani yake.[a] **12** Lakini mwishowe aling'olewa kwa ghadhabu.[b] Akatupwa chini, na kulikuwa na upepo wa mashariki ulioyakausha matunda yake.[c] Fimbo yake yenye nguvu ilikatwa nayo ikakauka.[d] Moto wenyewe ukaiteketeza.[e] **13** Na sasa amepandwa nyikani,[f] katika nchi isiyo na maji na yenye kiu.[g] **14** Na moto ukatoka katika fimbo yake.[h] Ukateketeza machipukizi yake, matunda yake, na ndani yake akawa hana fimbo yoyote yenye nguvu, fimbo yoyote ya enzi ya kutawalia.[i]

"'Huo ni wimbo wa huzuni, nao utakuwa wimbo wa huzuni.'"[j]

20 Ikawa kwamba katika mwaka wa saba, katika mwezi wa tano, siku ya kumi ya mwezi huo, baadhi ya watu kati ya wazee wa Israeli wakaja kuuliza juu ya Yehova,[k] nao wakaketi mbele yangu.[l] **2** Ndipo neno la Yehova likanijia, na kusema: **3** "Mwana wa binadamu, sema na wanaume wazee wa Israeli, nawe utawaambia, 'Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: "Je, mnakuja kuuliza neno juu yangu?[m] 'Kama ninavyoishi, hamtauliza neno juu yangu,'[n] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."'

4 "Je, utawahukumu? Je, utawahukumu, Ee mwana wa binadamu?[o] Wajulishe machukizo ya mababu zao.[p] **5** Nawe

SURA 19

a 2Fa 23:33; 2Nya 36:4; Yer 22:11
b 2Fa 23:34
c 2Nya 36:5; Yer 22:17
d 2Fa 24:4
e Eze 12:19
f Met 19:12; Met 28:15; Eze 22:25
g 2Fa 24:2
h Eze 12:13; Eze 17:20
i Omb 4:20
j 2Fa 24:12
k Eze 6:2
l Ho 2:2
m Zb 80:8; Isa 5:1; Eze 15:2; Eze 17:6
n Hes 24:6; Kum 8:7
o Hes 24:17; Ezr 4:20

Safu ya 2

a Eze 31:3; Da 4:11
b Isa 5:5; Yer 17:10; Yer 31:28; Eze 15:6
c Ho 13:15
d 2Fa 23:34; 2Fa 24:6; 2Fa 25:6
e Kum 32:22; Eze 15:4
f Kum 28:48; Yer 17:6; Yer 52:27
g Yer 9:11
h Amu 9:15; 2Fa 24:20
i Ne 9:37; Eze 17:18; Eze 21:26
j Omb 4:20

SURA 20

k Eze 8:1
l Eze 14:1
m Isa 1:12
n 1Sa 28:6; Met 15:8; Met 28:9; Isa 1:15; Eze 14:3; Mik 3:7
o Eze 14:4
p Eze 16:2; Eze 16:51; Eze 22:2; Eze 23:36; Lu 11:47; Mdo 7:51

utawaambia, ‘Hivi ndivyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema: “Katika siku ile nilipochagua Israeli,[a] pia niliuinua mkono[b] wangu katika kiapo kwa uzao wa nyumba ya Yakobo[c] na kujijulisha kwao katika nchi ya Misri.[d] Naam, niliuinua mkono wangu katika kiapo kwao, na kusema, ‘Mimi ni Yehova Mungu wenu.’[e] **6** Katika siku hiyo niliuinua mkono[f] katika kiapo kwao ili kuwatoa katika nchi ya Misri mpaka katika nchi niliyokuwa nimeipeleleza kwa ajili yao, yenye kutiririka maziwa na asali.[g] Hiyo ilikuwa ni pambo la nchi zote.[h] **7** Nami nikaendelea kuwaambia, ‘Tupilieni mbali, kila mmoja wenu, machukizo ya macho yake,[i] nanyi msijitie unajisi kwa sanamu za mavi za Misri.[j] Mimi ni Yehova Mungu wenu.’[k]

8 “‘“Nao wakaanza kuniasi,[l] wala hawakukubali kunisikiliza. Kila mmoja wao hakuyatupilia mbali machukizo ya macho yake, nazo sanamu zao za mavi za Misri hawakuziacha,[m] hivi kwamba nikaahidi kumwaga ghadhabu yangu juu yao, ili kuitimiliza hasira yangu juu yao katikati ya nchi ya Misri.[n] **9** Nami nikachukua hatua kwa ajili ya jina langu mwenyewe ili lisitiwe unajisi mbele ya macho ya mataifa ambayo walikuwa katikati yao,[o] kwa sababu nilikuwa nimejijulisha kwao mbele ya macho yao kwa kuwatoa katika nchi ya Misri.[p] **10** Kwa hiyo nikawatoa katika nchi ya Misri na kuwaingiza nyikani.[q]

11 “‘“Nami nikawapa sheria[r] zangu; nayo maamuzi yangu ya hukumu[a] nikawajulisha, ili mtu ambaye huendelea kuyafanya aweze pia kuishi kwa hayo.[b] **12** Nami nikawapa pia sabato zangu,[c] ziwe ishara kati yangu nao,[d] ili wajue kwamba mimi ni Yehova ninayewatakasa.

13 “‘“Lakini wao, nyumba ya Israeli, waliniasi nyikani.[e] Hawakutembea katika sheria[f] zangu, nao wakayakataa maamuzi yangu ya hukumu,[g] ambayo, mtu akiendelea kuyafanya, pia ataendelea kuishi kwa hayo.[h] Nazo sabato zangu walizitia unajisi sana,[i] hivi kwamba nikaahidi kumwaga ghadhabu yangu juu yao nyikani, ili kuwaangamiza.[j] **14** Lakini nilitenda kwa ajili ya jina langu mwenyewe ili lisitiwe unajisi mbele ya macho ya mataifa, ambao nilikuwa nimewatoa mbele ya macho yao.[k] **15** Na mimi mwenyewe pia nikawainulia mkono wangu katika kiapo nyikani,[l] kwamba sitawaingiza katika nchi niliyokuwa nimeitoa, yenye kutiririka maziwa na asali,[m] (hiyo ni pambo la nchi zote,)[n] **16** kwa sababu walikataa maamuzi yangu mwenyewe ya hukumu; nazo sheria zangu, hawakutembea katika hizo, nazo sabato zangu walizitia unajisi, kwa sababu moyo wao ulikuwa ukifuatilia sanamu zao za mavi.[o]

17 “‘“Nalo jicho langu likaanza kuwasikitikia ili kunizuia nisiwaharibu,[p] nami sikuwaangamiza nyikani. **18** Nami nikawaambia wana wao nyikani,[q] ‘Msitembee katika ma-

SURA 20
a Kut 6:7; Kum 7:6; Isa 41:8
b Isa 62:8
c Kut 6:8; Kum 32:40; Eze 47:14
d Kut 3:8; Kut 4:31; Kum 4:34; Zb 103:7
e Kut 20:2
f Ebr 6:13
g Kut 3:8; Kum 6:3; Kum 8:7; Yos 5:6; Yer 11:5; Yer 32:22
h Zb 48:2; Da 8:9; Da 11:41; Zek 7:14
i 2Nya 15:8; Eze 18:31
j Law 17:7; Law 18:3; Kum 29:17; Yos 24:14
k Kut 16:12; Law 11:44; Law 20:7
l Kum 9:7; 1Sa 15:23; Ne 9:26; Isa 63:10
m Kut 32:4
n Yos 24:14; Eze 7:8
o Kut 32:12; Hes 14:13; Kum 9:28; Yos 7:9; 1Sa 12:22
p Yos 2:10; Yos 9:9; 1Sa 4:8
q Kut 13:17; Kut 15:22
r Law 3:17

Safu ya 2
a Kum 4:8; Ne 9:13; Zb 147:19
b Kum 8:3; Kum 30:16; Lu 10:28; Ro 10:5; Ga 3:12
c Kut 20:8; Law 23:3; Law 23:24; Law 23:32; Law 25:4; Law 25:11; Kum 5:12; Ne 9:14
d Kut 13:9; Kut 31:13; Kut 35:2
e Kut 32:8; Hes 14:22; Zb 78:40; Zb 95:8
f Law 26:15
g Law 26:43; Met 1:25; Eze 16:24
h Eze 18:9; Ro 10:5
i Isa 56:6
j Hes 14:12
k Yos 7:9; Eze 36:22

l Hes 14:30; Zb 95:11; Zb 106:26; m Law 20:24; Hes 13:27; n Zek 7:14; o Kut 32:4; Hes 15:39; Hes 25:2; 1Fa 21:26; Eze 14:4; Mdo 7:42; p Ne 9:19; Zb 78:38; Yer 30:11; Omb 3:22; q Hes 14:33.

sharti ya mababu zenu,[a] wala
msizishike hukumu zao,[b] wala
msijitie unajisi kwa sanamu
zao za mavi.[c] **19** Mimi ni Ye-
hova Mungu wenu.[d] Tembee-
ni katika sheria[e] zangu mwe-
nyewe, na kuyashika maamuzi
yangu mwenyewe ya hukumu[f]
na kuyafanya.[g] **20** Na zitaka-
seni sabato zangu mwenyewe,[h]
nazo zitakuwa ishara kati ya-
ngu na ninyi, ili mjue kwamba
mimi ni Yehova Mungu wenu.'[i]
21 "'"Na hao wana wakaa-
nza kuniasi.[j] Hawakute-
mbea katika sheria zangu,
nayo maamuzi yangu ya hu-
kumu hawakuendelea kuya-
shika kwa kuyafanya, amba-
yo, kama mtu akiendelea ku-
yafanya, ataendelea pia ku-
ishi kwa hayo.[k] Sabato zangu
walizitia unajisi.[l] Kwa hiyo
nikaahidi kumwaga ghadha-
bu yangu juu yao, ili kuitimi-
liza hasira yangu juu yao nyi-
kani.[m] **22** Nami nikaurudi-
sha mkono wangu[n] na kutenda
kwa ajili ya jina langu mwe-
nyewe, ili lisitiwe unajisi mbe-
le ya macho ya mataifa, ambao
nilikuwa nimewatoa mbele
ya macho yao.[o] **23** Pia, mimi
mwenyewe niliwainulia mko-
no wangu katika kiapo nyika-
ni,[p] ili kuwatawanya kati ya
mataifa na kuwatawanya kati
ya nchi mbalimbali,[q] **24** kwa
sababu hawakufanya maamu-
zi yangu mwenyewe ya huku-
mu[r] nao walizikataa sheria za-
ngu mwenyewe[s] nao wakazitia
unajisi sabato zangu mwenye-
we,[t] nayo macho yao yalizi-
fuata sanamu za mavi za ma-
babu zao.[u] **25** Na mimi mwe-
nyewe pia niliwaacha wawe na
masharti ambayo hayakuwa

SURA 20

a Zb 78:8
Eze 5:7
b Mdo 7:51
1Pe 1:18
c Yer 2:7
d Kum 5:6
Zb 81:10
e Law 25:18
Kum 5:32
f Kum 4:1
g Kum 5:1
h Yer 17:22
i Kut 31:13
j Hes 25:1
Kum 9:23
1Fa 13:21
k Eze 20:11
l Eze 20:13
m 1Sa 12:15
1Sa 15:23
Zb 5:10
Isa 1:20
Isa 63:10
Eze 7:8
n Zb 78:38
o Zb 25:11
Zb 79:9
Yer 14:7
Da 9:19
p Kum 32:40
q Law 26:33
Kum 28:64
Zb 106:27
Yer 15:4
r Law 26:43
s Law 26:15
t Eze 20:13
u Yer 2:7
Yer 3:9
Eze 6:9

Safu ya 2

a Zb 81:12
Isa 66:4
Ro 1:24
2Th 2:11
b Law 18:21
2Fa 16:3
2Fa 17:17
2Fa 21:6
2Nya 28:3
2Nya 33:6
Yer 7:31
Yer 19:5
Yer 32:35
Eze 16:20
c Eze 6:7
d Eze 2:7
e Ro 2:24
f Yos 23:5
Ne 9:22
g Zb 105:9
Eze 20:6
h Kum 12:2
1Fa 14:23
Isa 65:7
Yer 2:20
i Zb 78:58
Isa 57:5
Eze 6:13
j Eze 16:19
k Yer 19:13
l Eze 16:24
m Hes 32:14
n Amu 2:19
2Nya 21:13
Yer 7:28
Yer 13:27
Mdo 7:51

mazuri na maamuzi ya huku-
mu ambayo hawangeweza kue-
ndelea kuishi kulingana nayo.[a]
26 Nami nikawa nikiwaacha
watiwe unajisi kwa zawadi zao
walipomfanya kila mtoto ali-
yelifungua tumbo la uzazi api-
te katikati ya moto,[b] ili niwa-
fanye ukiwa, ili wapate kujua
kwamba mimi ni Yehova."'[c]
27 "Kwa hiyo sema na nyu-
mba ya Israeli, Ee mwana wa
binadamu, nawe utawaam-
bia hivi,[d] 'Hivi ndivyo Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yeho-
va amesema: "Hata katika ha-
bari hii, mababu zenu wali-
sema vibaya juu yangu, kwa
kunitendea kwa ukosefu wa
uaminifu.[e] **28** Nami nikawa-
leta katika nchi[f] ambayo ni-
likuwa nimeuinua mkono wa-
ngu katika kiapo kwamba nita-
wapa wao.[g] Walipoona kila ki-
lima kilichoinuka[h] na kila mti
wenye matawi mengi, ndipo
wakaanza kutoa dhabihu[i] zao
huko na kutolea huko mato-
leo yao yenye kuudhi, na ku-
tolea huko harufu zao za kutu-
liza[j] na kumimina huko mato-
leo yao ya kinywaji.[k] **29** Kwa
hiyo nikawaambia, 'Mahali pa
juu mnapokuja panamaani-
sha nini, hivi kwamba paitwe
jina lake Mahali pa Juu mpaka
leo hii?'"'[l]
30 "Kwa hiyo iambie nyu-
mba ya Israeli, 'Hivi ndivyo
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova amesema: "Je, ninyi mna-
jitia unajisi katika njia za ma-
babu zenu,[m] na je, katika kufu-
atilia machukizo yao mnaingi-
lia kufanya uasherati?[n] **31** Na
katika kuinua zawadi zenu kwa
kuwafanya wana wenu wapite

katikati ya moto,[a] je, mnajitia
unajisi kwa ajili ya sanamu zenu
zote za mavi mpaka leo hii?[b] Wa-
kati huohuo je, mtauliza neno
juu yangu, Ee nyumba ya Israe-
li?"'[c]

"'Kama ninavyoishi,' asema
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova, 'Hamtauliza juu yangu.[d]
32 Na kile kinachoingia katika
roho yenu[e] hakika hakitatukia,[f]
kwa kuwa mnasema: "Na tuwe
kama mataifa, kama familia
za nchi mbalimbali,[g] katika
kuhudumia miti na mawe."'"[h]
33 "'Kama ninavyoishi,' ase-
ma Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova, 'nitatawala nikiwa mfa-
lme juu yenu kwa mkono we-
nye nguvu na kwa mkono ulio-
nyooshwa[i] na kwa ghadhabu ili-
yomwagwa.[j] **34** Nami nitawa-
toa kati ya vikundi vya watu,
nami nitawakusanya pamoja
kutoka katika nchi ambako
mmetawanywa kwa mkono
wenye nguvu na kwa mkono
ulionyooshwa na kwa ghadha-
bu iliyomwagwa.[k] **35** Nami
nitawaleta katika nyika ya vi-
kundi vya watu[l] na kujiweka
katika hukumu pamoja nanyi
huko uso kwa uso.[m]
36 "'Kama vile nilivyojiwe-
ka mwenyewe katika hukumu
pamoja na mababu zenu katika
nyika ya nchi ya Misri,[n] ndivyo
nitakavyojiweka mwenyewe
katika hukumu pamoja nanyi,'
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova. **37** 'Nami nita-
wafanya mpite chini ya fimbo[o]
na kuwaingiza katika kifu-
ngo cha agano.[p] **38** Nami ni-
tasafishia mbali kutoka kwenu
wale wanaoasi na wale wana-
onikosea,[q] kwa maana kutoka

SURA 20

a Kum 18:10
Zb 106:37
Yer 7:31
b Kum 29:17
1Fa 21:26
Eze 20:7
c 1Sa 28:6
Met 1:28
Isa 1:15
d Zek 7:13
e Eze 11:5
f Met 19:21
Omb 3:37
g Ro 12:2
h Kum 4:28
Kum 28:36
Yer 44:17
i Isa 40:10
j Yer 21:5
Eze 8:18
k Isa 27:13
Eze 34:16
Amo 9:9
l Ho 2:14
Mik 4:10
m Yer 2:9
Yer 25:31
Eze 17:20
Ho 4:1
n 1Ko 10:9
o Law 27:32
Yer 33:13
Eze 34:17
p Zb 89:34
q Hes 14:30
Eze 34:20
Mal 3:3
Mt 3:12

Safu ya 2

a Eze 13:9
b Zb 9:16
Eze 6:13
c Amu 10:14
Zb 81:12
Amo 4:4
d Met 21:27
Isa 1:13
Yer 7:10
Eze 23:39
e Isa 2:2
Isa 66:20
Eze 17:23
Mik 4:1
f Isa 56:7
Mik 4:2
Zek 8:22
g Mal 3:4
Ro 12:1
Ebr 13:15
h Mwa 8:21
Efe 5:2
Flp 4:18
i Isa 11:11
Yer 23:3
2Ko 6:17
j Isa 5:16
Eze 38:23
k Yer 24:7
Eze 36:23
l Eze 11:17
Eze 37:12
m Law 26:40
Ne 1:9
Eze 16:61
Ho 5:15
n Eze 6:9

katika nchi ya makao yao ya ki-
geni nitawaleta, lakini hawata-
kuja kwenye udongo wa Israe-
li;[a] nanyi mtalazimika kujua
kwamba mimi ni Yehova.'[b]
39 "Nanyi, Ee nyumba ya
Israeli, hivi ndivyo Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova
amesema, 'Nendeni kila mmo-
ja wenu akazitumikie sana-
mu zake mwenyewe za mavi.[c]
Na baadaye ikiwa hamnisiki-
lizi, basi hamtaendelea kuli-
tia unajisi jina langu takatifu
kwa zawadi zenu na kwa sana-
mu zenu za mavi.'[d]
40 "'Kwa maana katika mli-
ma wangu mtakatifu, katika
mlima wa kilele cha Israeli,'[e]
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova, 'huko ndiko wao,
nyumba yote ya Israeli ikiwa
nzima, itanitumikia, katika
nchi ile.[f] Nitafurahishwa nao
huko, na huko nitaitaka mi-
chango yenu na matunda ya
kwanza ya matoleo yenu ka-
tika vitu vyenu vyote vilivyo
vitakatifu.[g] **41** Kwa sababu
ya harufu ya kutuliza nitafu-
rahishwa nanyi,[h] nitakapowa-
toa kati ya vikundi vya watu
nami hakika niwakusanye pa-
moja kutoka katika nchi amba-
zo mmetawanywa,[i] nami ni-
tatakaswa ndani yenu mbele
ya macho ya mataifa.'[j]
42 "'Nanyi mtalazimika ku-
jua kwamba mimi ni Yehova,[k]
nitakapowaleta kwenye udo-
ngo wa Israeli,[l] katika nchi
ambayo niliuinua mkono wa-
ngu katika kiapo kwamba ni-
tawapa mababu zenu. **43** Na-
nyi hakika mtakumbuka huko
njia zenu na matendo yenu
yote[m] ambayo mlijitia unajisi
kwa hayo,[n] nanyi hakika mta-

jichukia mbele ya nyuso zenu
wenyewe kwa sababu ya ma-
mbo yenu yote mabaya ambayo
mliyatenda.[a] **44** Nanyi mta-
lazimika kujua kwamba mimi
ni Yehova[b] nitakapochukua
hatua kuhusiana nanyi kwa
ajili ya jina langu,[c] si kulinga-
na na njia zenu mbaya au ku-
lingana na matendo yenu ye-
nye uharibifu,[d] Ee nyumba ya
Israeli,' asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova."

45 Nalo neno la Yehova li-
kaendelea kunijia, na kuse-
ma: **46** "Mwana wa binada-
mu, elekeza uso[e] wako upande
wa eneo la kusini na udondo-
she[f] maneno kuelekea kusini,
na utoe unabii kwa msitu wa
uwanja wa kusini. **47** Nawe
utauambia msitu wa kusini,
'Sikia neno la Yehova. Hivi
ndivyo Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema: "Taza-
ma, ninawasha moto juu yako,[g]
nao utateketeza ndani yako
kila mti ambao ungali mbichi
na kila mti uliokauka.[h] Mwa-
li huo wa moto unaowaka ha-
utazimwa,[i] na kwa huo nyuso
zote zitateketezwa kutoka ku-
sini mpaka kaskazini.[j] **48** Na
watu wote wenye mwili wataona
kwamba mimi mwenyewe,
Yehova, nimeuwasha moto, ili
usipate kuzimwa."'"[k]

49 Nami nikasema: "Ole wa-
ngu, Ee Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova! Wanasema juu ya-
ngu, 'Je, yeye hatungi maneno
ya kimethali?'"[l]

21 Nalo neno la Yehova li-
kaendelea kunijia, na
kusema: **2** "Mwana wa bina-
damu, elekeza uso wako Ye-
rusalemu na udondoshe[m] ma-

SURA 20

a Yer 31:18
b Eze 24:24
c Zb 79:9
Eze 36:22
d 1Ti 1:16
e Eze 6:2
f Eze 21:2
Amo 7:16
g Kum 32:22
Yer 21:14
h Eze 17:24
Lu 23:31
i Isa 66:24
Mt 3:12
j Eze 21:4
k Kum 29:24
2Nya 7:20
Omb 2:17
l Eze 17:2

SURA 21

m Amo 7:16

Safu ya 2

a Eze 6:3
b Eze 12:19
Eze 20:42
c Eze 5:8
d Law 26:33
Eze 14:17
e Ayu 9:22
f Eze 7:2
Eze 20:47
g Kum 29:24
1Fa 9:7
Zb 9:16
h Isa 45:23
Yer 23:20
Nah 1:9
i Zb 69:23
Eze 29:7
j Isa 22:4
Yer 4:19
Eze 9:8
k Eze 24:19
l 2Fa 21:12
m Yer 6:22
n Yos 2:11
Yos 5:1
o Eze 7:17
p Eze 7:12
1Pe 4:7
q Isa 66:16
Yer 12:12
Amo 9:4
r Zb 7:12
s Yer 46:4

neno kuelekea mahali pata-
katifu,[a] na kutoa unabii juu ya
udongo wa Israeli.[b] **3** Nawe
utauambia udongo wa Israeli,
'Yehova amesema hivi: "Taza-
ma, niko juu yako,[c] nami ni-
tauchomoa upanga wangu
katika ala[d] yake na kumkati-
lia mbali kutoka kwako mwa-
dilifu na mwovu.[e] **4** Ili kwa
kweli nimkatilie mbali kutoka
kwako mwadilifu na mwovu,
kwa hiyo upanga wangu uta-
toka katika ala yake uwe juu ya
wote wenye mwili kutoka ku-
sini mpaka kaskazini.[f] **5** Nao
wote wenye mwili watalazimi-
ka kujua kwamba mimi mwe-
nyewe, Yehova, nimeuchomoa
upanga wangu kutoka katika
ala yake.[g] Hautarudi tena ka-
mwe."'[h]

6 "Na wewe, Ee mwana wa
binadamu, ugua kwa viuno
vyenye kutikisika.[i] Unapaswa
kuugua kwa uchungu mbele
ya macho yao.[j] **7** Na itakuwa
kwamba, ikiwa watakuambia
'Kwa nini unaugua?'[k] utase-
ma, 'Kwa sababu ya habari fu-
lani.'[l] Kwa maana hakika ita-
kuja,[m] na kila moyo utayeyu-
ka[n] na mikono yote itaanguka
chini na kila roho itahuzunika
na magoti yote yatadondoka
maji.[o] 'Tazama! Hakika itaku-
ja[p] na kutokezwa,' asema Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova."

8 Nalo neno la Yehova li-
kaendelea kunijia, na kuse-
ma: **9** "Mwana wa binadamu,
toa unabii, nawe useme, 'Yeho-
va amesema hivi: "Sema, 'Upa-
nga, upanga![q] Umenolewa,[r] nao
umesuguliwa pia. **10** Umeno-
lewa ili kupanga uchinjaji;
umesuguliwa ili upate kumeta-
meta.'"'"[s]

"Au je, tufurahi?"[a]

"'Je, huo unaikataa fimbo ya enzi[b] ya mwana wangu mwenyewe,[c] kama unavyoukataa kila mti?[d]

11 "'Na mtu huutoa usuguliwe, ili kuutumia kwa mkono. Huo—upanga umenolewa, na huo—huo umesuguliwa, ili kuutia mkononi mwa muuaji.[e]

12 "'Paaza kilio na kupiga mayowe,[f] Ee mwana wa binadamu, kwa maana huo wenyewe umekuja kuwa juu ya watu wangu;[g] huo uko juu ya wakuu wote wa Israeli.[h] Wale waliotupwa kwenye upanga wamekuwa pamoja na watu wangu.[i] Kwa hiyo piga paja kofi.[j] **13** Kwa maana uchunguzi umefanywa,[k] na vipi juu yake ikiwa unaikataa fimbo ya enzi pia?[l] Haitaendelea kuwapo,'[m] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

14 "Nawe, Ee mwana wa binadamu—toa unabii, na upige kiganja cha mkono juu ya kiganja cha mkono,[n] na 'Upanga!' unapaswa kurudiwa mara tatu.[o] Huo ni upanga wa walio-uawa. Ni upanga wa mtu mkuu aliyeuawa, unaowazunguka.[p] **15** Ili moyo uyeyuke[q] na ili kuzidisha wale walioshindwa katika malango yao yote,[r] nitafanya uchinjaji kwa upanga. Ole, huo umefanywa ili umetemete, umesuguliwa kwa ajili ya uchinjaji![s] **16** Jionyeshe kuwa na makali;[t] nenda upande wa kuume! Jipange mahali pako; nenda upande wa kushoto! Popote ambapo uso wako unaelekezwa! **17** Na mimi mwenyewe pia nitapiga kiganja changu kimoja cha mkono juu ya kile kiganja changu kingine cha mkono,[a] nami nitaituliza[b] ghadhabu[c] yangu. Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema."

18 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **19** "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, jipangie njia mbili ili upanga wa mfalme wa Babiloni uingie.[d] Zote mbili zinapaswa kutoka katika nchi moja, na uchonge mkono wa ishara;[e] uuchonge penye kichwa cha njia ya kwenda jijini. **20** Unapaswa kuweka njia ili upanga uingie ndani ya Raba[f] la wana wa Amoni, na moja ndani ya Yuda, ndani ya Yerusalemu lenye ngome.[g] **21** Kwa maana mfalme wa Babiloni alisimama tuli katika makutano ya njia, penye kichwa cha zile njia mbili, ili kufanya uaguzi.[h] Ametikisa mishale. Ameuliza habari kwa kutumia terafimu;[i] ametazama ndani ya ini. **22** Katika mkono wake wa kuume uaguzi ulikuwa kwa ajili ya Yerusalemu, ili kuweka mitambo ya kubomolea,[j] kufungua kinywa cha mtu kwa ajili ya uchinjaji, kupaaza sauti ya king'ora,[k] kuweka mitambo ya kubomolea juu ya malango, kujenga boma la kuzingira, kujenga ukuta wa kuzingira.[l] **23** Na hilo limekuwa kwao kama uaguzi usio wa kweli machoni pao[m]—wale ambao wameapishwa kwa viapo kwao;[n] naye analikumbuka kosa,[o] ili wao wakamatwe.[p]

24 "Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Kwa sababu mlifanya kosa lenu likumbukwe kupitia kufunuliwa kwa ukosaji wenu, ili dhambi zenu zionekane kulingana na matendo yenu yote, kwa sababu ya ninyi ku-

SURA 21

a Isa 5:14
b Mwa 49:10
c 2Sa 7:14
d Eze 19:11
e Yer 25:9
Yer 25:33
Yer 51:20
f Eze 9:8
Mik 1:8
g Yer 25:2
h Eze 19:1
i Yer 25:16
j Yer 31:19
k Yer 6:27
l 2Fa 25:7
Eze 19:14
m Yer 39:6
Eze 21:26
n Hes 24:10
Eze 6:11
o Law 26:21
p 2Fa 25:1
2Fa 25:2
Lu 19:43
q Eze 21:7
r Yer 17:27
s Eze 21:10
t Eze 14:17

Safu ya 2

a Eze 22:13
b Kum 28:63
Isa 1:24
Eze 16:42
c Eze 5:13
d Yer 1:10
e Eze 4:1
Eze 5:1
f Kum 3:11
Yer 49:2
Eze 25:5
Amo 1:14
g 2Sa 5:9
2Nya 26:9
2Nya 32:5
2Nya 33:14
Zb 48:12
Omb 4:12
h Hes 22:7
Kum 18:10
i Amu 18:14
2Fa 23:24
Zek 10:2
j 2Fa 25:1
Eze 4:2
k Yos 6:20
1Sa 17:20
l Yer 32:24
Yer 52:4
Eze 4:3
m Isa 28:15
n 2Nya 36:13
Eze 17:13
o 2Fa 24:20
Ayu 34:11
p 2Fa 25:6

kumbukwa[a] mtakamatwa kwa
mkono.’[b]
25 “Na wewe, Ee mwenye
majeraha kiasi cha kufisha,
mkuu[c] mwovu wa Israeli,[d]
ambaye siku yake imekuja katika wakati wa kosa la mwisho,[e]
26 Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova amesema hivi, ‘Kiondoe
kilemba, na kulivua taji.[f] Hili
halitakuwa tena kama lilivyo.[g]
Kiinue kilicho chini,[h] na ukishushe kilicho juu.[i] **27** Nitaliharibu, nitaliharibu, nitaliharibu.[j] Nalo hili pia, hakika hili
halitakuwa la mtu yeyote mpaka atakapokuja yule aliye na
haki ya kisheria,[k] nami nitampa yeye.’[l]
28 “Na wewe, Ee mwana wa
binadamu, toa unabii, nawe
useme, ‘Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi kuhusu wana wa Amoni na kuhusu shutuma kutoka kwao.’
Nawe useme, ‘Upanga, upanga umechomolewa kwa ajili ya uchinjaji, umesuguliwa ili
kuufanya uangamize, ili kumetameta,[m] **29** kwa sababu ya
wao kutazama kwa ajili yako
jambo lisilo halisi, kwa sababu
ya kukufanyia uaguzi wa uwongo,[n] ili kukuweka juu ya shingo za waliochinjwa, watu waovu ambao siku yao imekuja
katika wakati wa kosa la mwisho.[o] **30** Urudishe huo katika ala yake. Katika mahali ulipoumbwa wewe, katika nchi ya
asili yako,[p] nitakuhukumu.
31 Nami nitamwaga shutuma
zangu juu yako. Kwa moto
wa ghadhabu yangu nitapuliza juu yako,[q] nami nitakutia
mkononi mwa watu wasiotumia akili, mafundi wa uharibifu.[r] **32** Wewe utakuwa kuni

SURA 21

a Yer 2:34
b Yer 15:2
c 1Fa 11:34
d 2Nya 36:13
Yer 24:8
Yer 52:2
Eze 17:19
e Eze 7:6
f 2Fa 25:6
Yer 13:18
Yer 44:30
Yer 52:11
g Eze 21:13
h 1Sa 2:7
Zb 75:7
Zb 113:7
Da 4:17
Flp 2:9
i Yer 24:8
Eze 12:13
Da 4:37
Lu 21:24
j 2Nya 20:23
Eze 5:16
k Mwa 49:10
Zb 89:3
Zb 110:1
Isa 9:6
Isa 11:10
Eze 37:25
Lu 1:32
Ro 15:12
Ufu 5:5
l Zb 2:8
Da 7:14
Lu 22:29
m Yer 49:2
n Eze 12:24
Eze 22:28
o Zb 37:13
p Kum 3:11
q Yer 22:22
Yer 49:3
r Yer 4:7
Eze 25:5

Safu ya 2

a Yer 49:2
b Isa 55:11

SURA 22

c Eze 20:4
Eze 23:36
d 2Fa 21:16
Yer 2:34
Ho 4:2
Mt 23:37
e Isa 58:1
Eze 16:2
Eze 16:51
f Eze 24:6
g Eze 12:25
2Pe 2:3
h 2Fa 21:11
2Fa 23:24
i Mwa 9:6
2Fa 21:16
Zb 106:38
Eze 23:37
j Law 26:30
k Kum 28:37
1Fa 9:7
2Nya 7:20
Zb 79:4
Zb 80:6
Yer 18:16
Eze 5:14
Eze 23:32
Da 9:16
l Zb 79:4
m Isa 1:23
Eze 19:1
Mik 3:1
Sef 3:3
n Mik 2:1

kwa ajili ya moto.[a] Damu yako
mwenyewe itakuwa katikati
ya nchi. Hutakumbukwa, kwa
maana mimi mwenyewe, Yehova, nimesema.’ ”[b]

22 Nalo neno la Yehova lika-
endelea kunijia, na ku-
sema: **2** “Na wewe, Ee mwana
wa binadamu, je, utahukumu,[c]
je, utahukumu lile jiji lenye
hatia ya damu[d] na kulifanya
lijue machukizo yake yote?[e]
3 Nawe utasema, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: “Ee jiji, linalomwaga
damu[f] katikati yake mpaka wakati wake ufike,[g] na ambalo limefanya sanamu za mavi ndani yake ili kuwa lisilo safi,[h]
4 umekuwa na hatia kwa damu
yako ambayo umemwaga,[i] na
umekuwa usiye safi kwa sanamu zako za mavi ambazo umefanya.[j] Nawe unazileta siku
zako karibu, nawe utaifikia miaka yako. Ndiyo sababu lazima nikufanye kuwa kitu cha
kushutumiwa kwa mataifa na
cha kudhihakiwa katika nchi
zote.[k] **5** Nchi zilizo karibu
nawe na zile zilizo mbali nawe
zitakudhihaki, wewe uliye na
jina lisilo safi, uliyejaa mvurugo.[l] **6** Tazama! Wakuu[m] wa
Israeli wamekuwa ndani yako,
kila mmoja akiwa amejitoa
kwa mkono wake ili kumwaga
damu.[n] **7** Wamemtendea dharau baba na mama ndani yako.[o]
Wamemtendea mkaaji mgeni
ndani yako kwa upunjaji.[p] Wamewatendea vibaya mvulana
asiye na baba na mjane ndani
yako.” ’ ”[q]

o Kum 27:16; Met 20:20; p Kut 22:21; Met 22:22; q Zb 82:3; Zb 94:6; Isa 1:17; Yer 7:6; Zek 7:10; Mal 3:5.

8 "'Umepadharau mahali pangu patakatifu, nazo sabato zangu umezitia unajisi.[a] **9** Wachongezi wanaofanya hivyo waziwazi wamo ndani yako, kwa kusudi la kumwaga damu;[b] nao wamekula juu ya milima ndani yako.[c] Wameendeleza mwenendo mpotovu ndani yako.[d] **10** Wameufunua uchi wa baba ndani yako;[e] wamemfedhehesha mwanamke asiye safi katika hedhi yake ndani yako.[f] **11** Na mwanamume amefanya chukizo pamoja na mke wa mwenzake, na mwanamume amemnajisi[g] binti-mkwe wake mwenyewe kwa mwenendo mpotovu;[h] na ndani yako mwanamume amemfedhehesha dada yake, binti ya baba yake mwenyewe.[i] **12** Wamechukua rushwa ndani yako kwa kusudi la kumwaga damu.[j] Umechukua faida na riba,[k] nawe kwa ujeuri unaendelea kupata mapato[l] ya wenzako kwa upunjaji,[m] nawe umenisahau mimi,'[n] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

13 "'Na, tazama! Nimeupiga mkono wangu[o] kwa sababu ya pato lisilo la haki ambalo umepata,[p] na kwa sababu ya matendo yako ya kumwaga damu yaliyo katikati yako.[q] **14** Je, moyo wako utaendelea kuvumilia[r] au mikono yako kukupa nguvu katika siku ambayo nitatenda kukuelekea wewe?[s] Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema nami nitatenda.[t] **15** Nami nitakutawanya wewe kati ya mataifa na kukutawanya kati ya nchi[u] hizo, nami nitauharibu uchafu wako kutoka ndani yako.[v] **16** Nawe hakika utatiwa unajisi ndani yako mwenyewe mbele ya macho ya mataifa, nawe utalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.'"[a]

17 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **18** "Mwana wa binadamu, kwangu mimi wale wa nyumba ya Israeli wamekuwa kama takataka.[b] Wote ni shaba na bati na chuma na risasi katikati ya tanuru. Wamekuwa takataka nyingi, ile ya fedha.[c]

19 "Kwa hiyo, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Kwa sababu ninyi nyote mmekuwa kama takataka[d] nyingi, kwa hiyo, tazama, ninawakusanya ninyi pamoja katikati ya Yerusalemu.[e] **20** Kama kukusanya fedha na shaba na chuma[f] na risasi na bati katikati ya tanuru, ili kupuliza[g] juu yake kwa moto kusudi ziyeyuke,[h] ndivyo nitakavyowakusanya wao pamoja katika hasira yangu na katika ghadhabu yangu, nami nitawapuliza na kuwayeyusha ninyi. **21** Nami nitawakusanya pamoja na kupuliza juu yenu kwa moto wa ghadhabu yangu,[i] nanyi mtayeyushwa katikati yake.[j] **22** Kama kuyeyushwa kwa fedha katikati ya tanuru, ndivyo ninyi mtakavyoyeyushwa katikati yake; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimemwaga ghadhabu yangu juu yenu.'"[k]

23 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **24** "Mwana wa binadamu, iambie hivi, 'Wewe ni nchi isiyosafishwa, ambayo hainyeshewi wakati wa siku ya shutu-

SURA 22

a Law 19:30; Eze 20:13; Eze 23:38
b Kut 23:1; Law 19:16
c Eze 18:6
d Amu 20:6; Zb 26:10; Met 10:23; Yer 13:27; Eze 16:27; 2Pe 2:7
e Law 18:7; Law 20:11; Kum 27:20; 1Ko 5:1
f Law 18:19; Law 20:18
g Law 18:20; Law 20:10; Kum 22:22; Yer 5:8
h Law 18:15; Law 20:12; Eze 18:11
i Law 20:17; Kum 27:22; 2Sa 13:1
j Kut 23:8; Kum 16:19; Kum 27:25; Zb 26:9; Isa 1:23; Amo 5:12
k Kut 22:25; Law 25:36; Kum 23:19; Eze 18:13
l Met 1:19
m Law 6:2
n Kum 32:18; Zb 106:21
o Eze 21:17
p Met 28:8
q Eze 22:2
r Eze 21:7
s Ayu 40:9; 1Ko 10:22
t Eze 17:24
u Kum 4:27; Kum 28:25; Eze 12:15
v Isa 1:25; Eze 23:27; Mal 3:3

Safu ya 2

a Zb 9:16; Eze 6:7; Eze 6:13
b Isa 1:22; Yer 6:28
c Met 17:3; Isa 48:10; Yer 6:29
d Zb 119:119; Met 25:4
e Mik 4:12; Mt 13:30
f Ayu 28:2
g Isa 54:16; Yer 6:29
h Eze 21:31
i Kum 4:24; Zb 21:9; Isa 30:33; Yer 21:12; Eze 22:20
j Zb 68:2; Zb 112:10
k Eze 20:8; Ho 5:10

ma.[a] **25** Katikati yake kuna
hila ya manabii wake,[b] kama si-
mba anayenguruma, anayera-
rua mawindo.[c] Kwa kweli wa-
nairarua nafsi.[d] Wanaendelea
kuchukua hazina na vitu vye-
nye thamani.[e] Wamewazidisha
wajane wake katikati yake.[f]
26 Makuhani wake wenyewe
wameitendea jeuri sheria ya-
ngu,[g] nao wanaendelea kutia
unajisi mahali pangu patakatifu.[h] Hawatofautishi kati ya
kitu kitakatifu na cha kawa-
ida,[i] nao hawajafanya chocho-
te kijulikane kati ya kitu ki-
sicho safi na kilicho safi,[j] nao
wameyaficha macho[k] yao yasi-
one sabato zangu, nami ni-
natiwa unajisi katikati yao.[l]
27 Wakuu wake walio katikati
yake ni kama mbwa-mwitu wa-
naorarua mawindo katika ku-
mwaga damu,[m] katika kuanga-
miza nafsi kusudi wapate pato
lisilo la haki.[n] **28** Nao ma-
nabii wake wamewapigia lipu
kwa kutumia chokaa,[o] wakio-
na maono yasiyo halisi[p] na ku-
agua uwongo[q] kwa ajili yao, na
kusema: "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi,"
wakati ambapo Yehova mwe-
nyewe hajasema. **29** Watu
wa nchi wenyewe wameende-
sha mbinu ya kupunja[r] nao
wamenyakua katika unyang'a-
nyi,[s] nao wamemtendea viba-
ya[t] anayeteseka na aliye ma-
skini, na kumpunja bila haki
mkaaji mgeni.'[u]
30 "'Nami nikaendelea ku-
mtafuta mtu kati yao ambaye
angekuwa akiurekebisha ukuta wa mawe[v] na kusimama ka-
tika pengo[w] mbele yangu kwa
ajili ya nchi hiyo, ili mimi ni-
siiangamize;[x] nami sikumpa-
ta yeyote. **31** Kwa hiyo ni-
tamwaga shutuma[a] zangu juu
yao. Nitawaangamiza wao kwa
moto wa ghadhabu yangu.[b] Ni-
taileta njia yao juu ya kichwa
chao wenyewe,'[c] asema Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova."

23 Na neno la Yehova li-
kanijia,[d] na kusema:
2 "Mwana wa binadamu, kulikuwa na wanawake wawili, binti
za mama mmoja.[e] **3** Nao wa-
kaanza kufanya ukahaba katika Misri.[f] Wakati wa ujana wao
walifanya ukahaba.[g] Huko ma-
ziwa yao yalifinywa-finywa,[h] na
huko walivibana vifua vya ubikira wao. **4** Nayo majina yao ya-
likuwa Ohola, yule mkubwa na
Oholiba dada yake, nao waka-
ja kuwa wangu[i] na kuanza ku-
zaa wana na mabinti.[j] Nayo
majina yao, Ohola ni Samaria,[k]
na Oholiba ni Yerusalemu.[l]
5 "Naye Ohola akaanza kufa-
nya ukahaba,[m] alipokuwa chini
yangu, na kuendelea kuwa na
uchu kuwaelekea wale wanao-
mpenda kwa tamaa,[n] kuwaele-
kea Waashuru,[o] waliokuwa kari-
bu, **6** magavana waliovaa ma-
vazi ya bluu, na watawala-wa-
saidizi—wote wakiwa vijana
wenye kupendeza, askari we-
nye kupanda farasi. **7** Naye
akaendelea kuwagawia ukaha-
ba wake, wote wakiwa wana
bora wa Ashuru; na wale wote
ambao alikuwa na uchu ku-
waelekea—pamoja na sanamu
zao za mavi—alijitia unajisi.[p]
8 Na ukahaba wake uliotoka
Misri hakuuacha, kwa maana
walikuwa wamelala naye wa-
kati wa ujana wake, nao ndio

SURA 22
a Isa 10:5
b Yer 5:31
Yer 6:13
Ho 6:9
c Mik 3:5
d Mk 12:40
Lu 20:47
e Yak 5:4
f Yer 15:8
g Yer 2:8
Omb 4:13
Mik 3:11
Sef 3:4
Mal 2:8
h Law 20:3
Law 22:2
i Law 10:10
Eze 44:23
j Law 11:47
Mdo 10:14
k Eze 20:13
l Eze 36:20
Ro 2:24
m Mik 3:2
Sef 3:3
n Mt 21:13
o Isa 30:10
Eze 13:10
p Eze 21:29
q Kum 13:3
Yer 23:25
Omb 2:14
r Law 6:2
Isa 1:23
Yer 5:26
Yer 7:9
Yer 21:12
Mik 2:2
s Zb 62:10
Isa 3:14
t Kut 22:21
Law 19:33
u Kut 23:9
v Yer 5:1
w Zb 106:23
x Mwa 18:23
Kut 32:11

Safu ya 2
a Isa 26:20
b Isa 10:22
Nah 1:6
c Eze 11:21
Ro 2:6
Ga 6:7

SURA 23
d 2Pe 1:21
e Yer 3:7
f Law 17:7
Kum 29:17
Yos 24:14
Eze 20:8
g Eze 16:22
Ho 2:13
h Eze 23:21
i Kut 19:5
Yer 2:3
Eze 16:8
j Eze 16:20
Ga 4:25
k 1Fa 16:24
l 1Fa 8:29
m 1Fa 14:16
1Fa 21:26
2Fa 17:7
n Ho 2:5

o 2Fa 15:19; 2Fa 16:7; 2Fa 17:3; Yer 2:18; Yer 2:36; Omb 5:6; Eze 16:28; Ho 5:13; Ho 7:11; Ho 8:9; p Zb 106:39; Ho 5:3; Ho 6:10.

waliokuwa wamebana vifua vya
ubikira wake nao waliende-
lea kumimina juu yake uasherati wao.[a] **9** Kwa hiyo nilimtia mkononi mwa wale wanaompenda kwa tamaa,[b] mkononi mwa wana wa Ashuru, ambao alikuwa na uchu kuwaelekea.[c] **10** Hao ndio walioufunua uchi wake.[d] Wakawachukua wanawe na binti zake,[e] naye wakamuua kwa upanga. Akaja kuwa na sifa mbaya kwa wanawake, nao wakatekeleza matendo ya hukumu juu yake.

11 "Dada yake Oholiba alipoona jambo hilo,[f] basi akatimiza tamaa yake ya kimwili kwa uharibifu mkubwa kuliko yeye, na ukahaba wake mwingi kuliko uasherati wa dada yake.[g] **12** Akawa na uchu kuwaelekea wana wa Ashuru,[h] magavana na watawala-wasaidizi waliokuwa karibu, waliovaa mavazi yenye kupendeza, askari wenye kupanda farasi —wote wakiwa vijana wenye kupendeza.[i] **13** Nami nikaona jambo hilo, kwa sababu alikuwa amejitia unajisi, wote wawili walikuwa na njia moja.[j] **14** Naye akazidi kuongezea matendo yake ya ukahaba alipowaona wanaume waliochongwa ukutani,[k] sanamu[l] za Wakaldayo zilizochongwa na kupakwa rangi nyekundu,[m] **15** zilizofungwa mishipi[n] katika viuno vyao, zikiwa na vilemba vinavyoning'inia katika vichwa vyao, wote wakiwa na sura ya mashujaa wa vita, wanaofanana na wana wa Babiloni, wakiwa ni wazaliwa wa nchi ya Wakaldayo. **16** Naye akaanza kuwa na uchu kuwaelekea alipoona kwa macho[a] yake, naye akatuma wajumbe kwao katika Ukaldayo.[b] **17** Nao wana wa Babiloni wakaendelea kumjia, kwenye kitanda cha wonyesho wa upendo, na kumtia unajisi kwa uasherati wao;[c] nao wakaendelea kumtia unajisi, nayo nafsi yake ikaanza kugeukia mbali nao kwa kuchukizwa.

18 "Naye akaendelea kufunua matendo yake ya ukahaba na kufunua uchi wake,[d] hivi kwamba nafsi yangu ikageukia mbali kwa kuchukizwa isiandamane naye, kama vile nafsi yangu ilivyogeukia mbali kwa kuchukizwa isiandamane na dada yake.[e] **19** naye akaendelea kuzidisha matendo yake ya ukahaba[f] kufikia hatua ya kurudisha kumbukumbu ya siku za ujana wake,[g] wakati ambapo alifanya ukahaba katika nchi ya Misri.[h] **20** Naye akaendelea kuwa na uchu kama masuria wa wale ambao kiungo chao ni kama kiungo cha punda-dume na ambao kiungo chao cha uzazi ni kama kiungo cha uzazi cha farasi-dume.[i] **21** Nawe ukaendelea kuukazia fikira mwenendo mpotovu wa ujana wako kwa kufinywa kwa vifua vyako kutoka Misri[j] na kuendelea, kwa ajili ya maziwa ya ujana wako.[k]

22 "Kwa hiyo, Ee Oholiba, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Tazama, ninawaamsha juu yako wale wanaokupenda kwa tamaa,[l] wale ambao nafsi yako imegeukia mbali kutoka kwao ikiwa imechukizwa, nami nitawaleta juu yako pande zote,[m]

SURA 23

a Kut 32:4
1Fa 12:28
2Fa 10:29
2Fa 17:16
b 2Fa 15:29
c 2Fa 17:23
1Nya 5:26
d Eze 16:37
Ho 2:10
e 2Fa 17:6
2Fa 18:11
f Yer 3:7
g Yer 3:8
Eze 16:47
h 2Fa 16:7
2Nya 28:16
i Eze 23:6
j 2Fa 17:19
k Eze 8:10
l Yer 50:2
m Yer 22:14
n 1Sa 18:4

Safu ya 2

a Zb 119:37
Mt 5:28
1Yo 2:16
b Eze 16:29
c Eze 16:37
d Yer 3:2
Eze 16:36
e Kum 32:19
Zb 78:59
Zb 106:40
Yer 6:8
Yer 12:8
f Eze 16:25
Amo 4:4
g Eze 16:22
h Eze 20:7
i Eze 16:26
j Yos 24:14
k Eze 23:3
l Isa 10:5
Eze 16:37
Hab 1:6
Ufu 17:16
m Yer 6:22
Yer 12:9

23 wana wa Babiloni[a] na Wakaldayo[b] wote, Pekodi[c] na Shoa
na Koa, wana wote wa Ashu-
ru pamoja nao, vijana wenye
kupendeza, magavana na wa-
tawala-wasaidizi wote, mashu-
jaa wa vita na walioitwa, wote
wakiwa wamepanda farasi.
24 Nao lazima wataingia nda-
ni juu yako pamoja na kelele
za magari ya vita na za magu-
rudumu,[d] na pamoja na kuta-
niko la vikundi vya watu, pa-
moja na ngao kubwa na ngao
ndogo na kofia. Watajipanga
juu yako pande zote, nami ni-
tawapa hukumu, nao wata-
kuhukumu wewe kwa huku-
mu zao.[e] **25** Nami nitaonye-
sha ukali wangu juu yako,[f] nao
watakuchukulia hatua kati-
ka ghadhabu.[g] Wataondoa pua
yako na masikio yako, na se-
hemu yako inayobaki itaangu-
ka kwa upanga. Wao wenye-
we watawachukua wana wako
na binti zako,[h] na sehemu yako
inayobaki itateketezwa kwa
moto.[i] **26** Nao hakika wata-
kuvua mavazi[j] yako na ku-
vichukua vyombo vyako vi-
navyopendeza.[k] **27** Nami ha-
kika nitaufanya mwenendo
wako mpotovu ukome kutoka
kwako,[l] na ukahaba wako ku-
toka nchi ya Misri;[m] nawe hu-
tainua macho yako kuwaele-
kea, nawe hutakumbuka Misri
tena.'

28 "Kwa maana Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova
amesema hivi, 'Tazama, ni-
nakutia mkononi mwa wale
ambao umewachukia, mkono-
ni mwa wale ambao kuto-
ka kwao nafsi yako imegeu-
kia mbali ikiwa imechukizwa.[n]
29 Nao watakuchukulia hatua
kwa chuki na kuchukua mali
zako zote ulizofanyia kazi na
kukuacha ukiwa uchi na
tupu;[a] nao utupu wa matendo
yako ya uasherati na mwene-
ndo wako mpotovu na mate-
ndo yako ya ukahaba utafunuli-
wa.[b] **30** Utafanyiwa mambo
hayo kwa sababu uliyafuata ma-
taifa kama kahaba,[c] kwa sababu
ulijitia unajisi kwa sanamu zao
za mavi.[d] **31** Umetembea kati-
ka njia ya dada yako;[e] nami
nitalazimika kukitia kikombe
chake mkononi mwako.'[f]

32 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi, 'Ki-
kombe cha dada yako utaki-
nywa, kile chenye kina na kipa-
na.[g] Utakuwa kitu cha kuche-
kwa na kudhihakiwa, kikombe
kilicho na mengi.[h] **33** Utajaa
ulevi na huzuni, kwa kikombe
cha mshangao na cha ukiwa,
kikombe cha dada yako Sama-
ria. **34** Nawe utalazimika ku-
kinywa na kukimaliza,[i] na vi-
gae vyake utavitafuna, na ma-
ziwa yako utayang'oa.[j] "Kwa
maana mimi mwenyewe nime-
sema," asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova.'

35 "Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amese-
ma hivi, 'Kwa sababu umeni-
sahau[k] nawe ulinitupa nyuma
ya mgongo wako,[l] basi wewe
mwenyewe pia chukua mwe-
nendo wako mpotovu na mate-
ndo yako ya ukahaba.'"

36 Na Yehova akaendelea ku-
niambia: "Mwana wa bina-
damu, je, utawahukumu[m] Ohol-
a na Oholiba[n] na kuwaambia
machukizo yao?[o] **37** Kwa ma-
ana wamefanya uzinzi[p] na
damu imo mikononi mwao,[q]

SURA 23
a 2Fa 20:14
Isa 39:3
Eze 21:19
b 2Fa 24:2
Isa 23:13
c Yer 50:21
d Yer 47:3
Eze 26:10
Nah 3:2
e 2Sa 24:14
Yer 39:5
f Kum 29:20
Eze 38:19
Sef 1:18
g Eze 16:38
h Eze 23:4
Ho 2:4
Ga 4:25
i Eze 15:7
Eze 20:47
Ufu 18:8
j Yer 13:22
Eze 16:39
Ho 2:3
Ufu 17:16
k Isa 3:18
Yer 4:30
Eze 16:11
l Isa 27:9
Eze 16:41
Eze 22:15
Zek 13:2
m Eze 23:3
Eze 23:19
n Yer 21:7
Yer 34:20

Safu ya 2
a Kum 28:51
Eze 16:39
b Eze 16:36
Eze 16:37
c Zb 106:35
Yer 2:18
Yer 16:11
Yer 22:9
Eze 6:9
d Eze 23:7
e Yer 3:8
Eze 16:47
f 2Fa 21:13
Zb 11:6
Yer 7:15
Yer 25:15
Da 9:12
g Isa 51:17
h Kum 28:37
1Fa 9:7
Omb 2:15
Eze 22:5
i Zb 75:8
Isa 51:17
j Isa 32:12
k Isa 17:10
Yer 2:32
Yer 3:21
Yer 13:25
l 1Fa 14:9
Ne 9:26
m Yer 1:10
n Eze 23:4
o Isa 58:1
Eze 16:2
Eze 20:4
Eze 22:2
p Ho 1:2
Yak 4:4
q Eze 16:38
Eze 22:2

nao wamefanya uzinzi na sanamu zao za mavi.[a] Na, mbali
na hayo, waliwafanya wana wao
waliokuwa wamenizalia wapite motoni kama chakula kwao.[b]
38 Tena, hili ndilo wamenifanyia: Wamepatia unajisi[c] patakatifu[d] pangu katika siku hiyo,
nazo sabato zangu wamezitia
unajisi.[e] **39** Nao walipokuwa
wamewachinja wana wao kwa
ajili ya sanamu zao za mavi[f]
waliingia ndani ya patakatifu
pangu katika siku hiyo ili kupatia unajisi,[g] na, tazama! hivyo
ndivyo wamefanya katikati ya
nyumba yangu.[h] **40** Tena, walipoanza kuwaita wanaume kutoka mbali, ambao walitumiwa mjumbe,[i] kisha, tazama! wao
wakaja,[j] kwa ajili ya yule ambaye ulikuwa umejiosha[k] kwa ajili yake, ukapaka rangi macho[l]
yako na kujipamba kwa mapambo.[m] **41** Nawe ukaketi juu
ya kitanda chenye utukufu,[n] pamoja na meza iliyowekwa kwa
utaratibu mbele yake,[o] nawe
ukaweka juu yake uvumba[p] wangu na mafuta[q] yangu. **42** Na
sauti ya umati uliostarehe ilikuwa ndani yake,[r] na kwa wanaume kutoka katika umati wa
wanadamu kulikuwa na walevi[s] wakiletwa kutoka nyikani,
nao wakaweka vikuku mikononi mwa wanawake na mataji yenye kupendeza juu ya vichwa
vyao.[t]
43 "Ndipo nikasema kuhusu
yule ambaye uzinzi[u] umemfanya
achakae, 'Sasa ataendelea kufanya ukahaba wake, naam, yeye
mwenyewe.'[v] **44** Nao wakaendelea kuingia kwake, kama
vile mtu anavyokuja kwa mwanamke kahaba; hivyo ndivyo walivyoingia kwa Ohola
na kwa Oholiba wakiwa wanawake wa mwenendo mpotovu.[a]
45 Lakini watu waadilifu,[b] hao
ndio watakaomhukumu kwa
hukumu ya wanawake wazinzi[c] na kwa hukumu ya wanawake wanaomwaga damu;[d]
kwa maana wao ni wanawake
wazinzi, na damu imo mikononi mwao.[e]
46 "Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Kutaniko litaletwa
juu yao[f] nao watafanywa kuwa
kitu chenye kutisha na kitu
cha kuporwa.[g] **47** Nalo kutaniko litawapiga kwa mawe,[h]
nao watakatwa kwa panga zao.
Watawaua wana wao na binti
zao,[i] nao wataziteketeza nyumba zao kwa moto.[j] **48** Nami
hakika nitafanya mwenendo
mpotovu[k] ukome nchini,[l] nao
wanawake wote watalazimika
kukubali kurekebishwa, hivi
kwamba wasifanye kulingana
na mwenendo wenu mpotovu.[m]
49 Nao watauleta mwenendo
wenu mpotovu juu yenu,[n] nanyi mtazichukua dhambi za sanamu zenu za mavi; nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi
ni Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova.'"[o]

24 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia katika mwaka wa tisa, katika mwezi wa kumi, siku ya
kumi ya mwezi huo, na kusema: **2** "Mwana wa binadamu,
jiandikie jina la siku hii, siku
hii ya leo. Mfalme wa Babiloni amejitupa juu ya Yerusalemu siku hii ya leo.[p] **3** Na utunge neno la kimethali kuhusu

SURA 23
a Eze 16:36
b Law 18:21
2Fa 17:17
Eze 16:20
c Yer 32:34
Eze 5:11
Eze 8:5
d 2Fa 21:4
e Ne 13:17
Eze 22:8
f Yer 7:31
g Law 20:3
Yer 7:11
h 2Nya 33:4
i Isa 57:9
j 2Fa 20:13
k Ru 3:3
Est 2:12
l 2Fa 9:30
Yer 4:30
m Met 7:10
Isa 3:18
Eze 16:13
n Est 1:6
Isa 57:7
Amo 2:8
Amo 6:4
o Isa 65:11
p Eze 8:11
q Met 7:17
Yer 44:17
Eze 16:18
Ho 2:8
r Kut 32:6
Ho 13:6
s Isa 28:1
t Eze 16:11
u Yak 4:4
v Ezr 9:7
Yer 13:23

Safu ya 2
a Eze 23:3
Eze 23:9
b Eze 14:14
Eze 14:20
c Law 20:10
Kum 22:21
Eze 16:38
d Mwa 9:6
Eze 23:37
e 2Fa 24:4
Zb 106:38
Isa 1:15
Ho 4:2
f Yer 25:9
Eze 16:40
g Yer 15:4
Yer 24:9
Yer 34:17
h Law 20:2
Eze 16:40
i 2Nya 36:17
j Kum 13:16
2Fa 25:9
Yer 39:8
Yer 52:13
k Amu 20:6
Eze 22:9
l Isa 26:9
m Kum 13:11
2Pe 2:6
n Isa 59:18
Eze 16:43
Ro 2:6
Ga 6:7
o Zb 9:16
Eze 6:13

SURA 24 p 2Fa 25:1; Yer 39:1; Yer 52:4.

nyumba hii yenye kuasi,[a] nawe
utasema kuwahusu,
"'Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova amesema hivi: "Tia mo-
toni chungu cha kupikia che-
nye mdomo mpana; kitie mo-
toni, na pia umimine maji nda-
ni yake.[b] **4** Kusanya vipande
ndani yake,[c] kila kipande che-
ma, paja na bega; kijaze mifu-
pa bora zaidi. **5** Kondoo bora
zaidi na achukuliwe,[d] na pia
urundike kuni zikiwa katika
mviringo chini yake. Tokosa vi-
pande vyake, pia upike mifupa
yake katikati yake."'"[e]
6 "Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amese-
ma hivi, 'Ole wake jiji lenye
matendo ya kumwaga damu,[f]
kile chungu cha kupikia che-
nye mdomo mpana, ambacho
kutu yake iko ndani yake, na
ambacho kutu yake haikukito-
ka! Kipande kwa kipande cha-
ke, kitoe nje;[g] kura yoyote isi-
pigwe juu yake.[h] **7** Kwa ma-
ana damu yake imekuwa kati-
kati yake kabisa.[i] Aliiweka juu
ya uso ulio wazi na wenye ku-
ng'aa, wa mwamba. Hakuimi-
mina chini, ili kuifunika kwa
mavumbi.[j] **8** Ili kuleta gha-
dhabu kwa ajili ya kulipiza ki-
sasi,[k] nimeiweka damu yake
juu ya uso ulio wazi na wenye
kung'aa, wa mwamba, ili isipa-
te kufunikwa.'[l]
9 "Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amesema
hivi, 'Ole wake jiji lenye mate-
ndo ya kumwaga damu![m] Mimi
mwenyewe pia nitalifanya fu-
ngu hilo liwe kubwa.[n] **10** Zi-
fanye kuni ziwe nyingi. Uwa-
she moto. Itokose nyama kabi-
sa. Na uumwage mchuzi mzi-

SURA 24
a Eze 17:12
Lu 8:10
b Yer 1:13
Eze 11:3
c Eze 11:7
d Yer 39:6
Eze 34:16
e Eze 24:10
f 2Fa 21:16
Eze 22:3
Mik 7:2
Mt 23:35
g Eze 11:7
Eze 11:9
h Yoe 3:3
Oba 11
Nah 3:10
i 1Fa 21:19
Yer 2:34
j Law 17:13
Kum 12:16
Isa 26:21
k Kum 32:35
Zb 94:1
l 2Fa 24:4
Yer 16:17
m Nah 3:1
Hab 2:12
Mt 23:37
n Isa 30:33

Safu ya 2
a Yer 21:10
Yer 32:29
Eze 22:15
b Eze 24:6
c Yer 5:3
Yer 6:29
d Amu 20:6
2Nya 36:14
Eze 22:9
2Pe 2:7
e Ayu 9:4
f Eze 5:13
Eze 8:18
g Hes 23:19
h Zb 33:9
i Yer 13:14
j Eze 5:11
Eze 9:10
k 1Sa 15:29
l Isa 3:11
Eze 16:43
Mt 16:27
Ro 2:6
m Kum 13:6
n Eze 24:18
Eze 24:21
Ho 4:9
o Kum 13:8
p Yer 16:5
q Law 10:6
r 2Sa 15:30
s Mik 3:7
t Yer 16:7

to, na uiache mifupa iwe moto
sana. **11** Kisimamishe juu ya
makaa yake ili kiwe moto; na
shaba yake itakuwa moto, nao
uchafu wake utayeyushwa ka-
tikati yake.[a] Kutu yake na ite-
ketee.[b] **12** Taabu! Zimemfa-
nya mtu achoke, lakini kiasi ki-
kubwa cha kutu yake hakito-
ki kwake.[c] Kutu yake na itiwe
motoni!'
13 "'Kulikuwa na mwenendo
mpotovu katika uchafu wako.[d]
Kwa sababu hiyo nililazimika
kukusafisha, lakini hukuwa safi
kutokana na uchafu wako.[e] Hu-
takuwa safi tena mpaka nitaka-
poituliza ghadhabu yangu kwa-
ko.[f] **14** Mimi mwenyewe, Ye-
hova, nimesema.[g] Lazima ije,[h]
nami nitatenda. Sitapuuza,[i]
wala sitasikitika[j] wala kujuta.[k]
Kulingana na njia zako na kuli-
ngana na matendo yako hakika
watakuhukumu,'[l] asema Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova."
15 Nalo neno la Yehova li-
kaendelea kunijia, kusema:
16 "Mwana wa binadamu, ta-
zama, ninaondolea mbali ku-
toka kwako kitu chenye ku-
tamanika[m] machoni pako kwa
pigo moja,[n] nawe usijipige ki-
fua, wala usilie, wala macho-
zi yako yasitoke.[o] **17** Ugua
pasipo maneno. Usiwaombole-
zee hata kidogo waliokufa.[p] Ji-
funge kitambaa chako cha ki-
chwani,[q] na uvae viatu vyako
miguuni[r] pako. Nawe usifuni-
ke masharubu,[s] wala usile mka-
te wa wanadamu."[t]
18 Nami nikasema na watu
asubuhi, naye mke wangu
mwishowe akafa jioni. Kwa
hiyo nilifanya asubuhi vile
ambavyo nilikuwa nimeamriwa.

19 Nao watu wakaendelea kuniambia: "Je, hutatuambia ni jinsi gani mambo haya yanatuhusu, mambo unayoyafanya?"[a] **20** Ndipo nikawaambia: "Neno la Yehova limenijia, na kusema, **21** 'Iambie nyumba ya Israeli: "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Tazama, mimi ninapatia unajisi patakatifu pangu,[b] fahari ya nguvu zenu,[c] kitu chenye kutamanika machoni penu[d] na kitu ambacho nafsi yenu hukihurumia, nao wana wenu na binti zenu ambao mmewaacha nyuma—wataanguka kwa upanga.[e] **22** Nanyi mtalazimika kufanya kama nilivyofanya. Hamtafunika masharubu,[f] wala kula mkate wa wanadamu.[g] **23** Nacho kitambaa chenu cha kichwa kitakuwa vichwani mwenu, navyo viatu vyenu vitakuwa miguuni penu. Hamtajipiga-piga wala hamtalia,[h] nanyi mtalazimika kuoza katika makosa yenu,[i] nanyi hakika mtaugua kila mtu pamoja na mwenzake.[j] **24** Na Ezekieli amekuwa ishara kwa ajili yenu.[k] Mtatenda kulingana na yote ambayo ametenda. Litakapokuja jambo hili,[l] ninyi pia mtalazimika kujua kwamba mimi ndiye Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.' " ' "[m]

25 "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, je, haitakuwa katika siku ambayo nitachukulia mbali ngome zao, kile kitu kizuri cha furaha yao, kitu chenye kutamanika machoni pao[n] na tamaa ya nafsi yao, wana wao na binti zao,[o] kwamba **26** katika siku hiyo mwenye kuponyoka atakujia ili kuyafanya masikio yasikie jambo hili?[a] **27** Katika siku hiyo kinywa chako kitafunguliwa kuelekea aliyeponyoka,[b] nawe utasema nawe hutakuwa bubu tena;[c] nawe hakika utakuwa ishara kwao,[d] nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova."[e]

25 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** "Mwana wa binadamu, elekeza uso wako kwa wana wa Amoni na kutoa unabii juu yao.[f] **3** Nawe utasema hivi kuwahusu wana wa Amoni, 'Sikieni neno la Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Kwa sababu umesema Aha! Juu ya patakatifu pangu, kwa sababu pametiwa unajisi, na juu ya nchi ya Israeli, kwa sababu imefanywa kuwa ukiwa, na juu ya nyumba ya Yuda, kwa sababu wameenda uhamishoni,[g] **4** kwa hiyo tazama, ninakutia wewe mkononi mwa Watu wa Mashariki uwe kitu cha kumilikiwa,[h] nao wataweka kambi zao zenye kuta ndani yako nao hakika wataweka ndani yako maskani zao. Wao wenyewe watakula matunda yako, nao wenyewe watakunywa maziwa yako.[i] **5** Nami nitafanya Raba[j] pawe kiwanja cha malisho cha ngamia na wana wa Amoni wawe mahali pa kupumzika kwa ajili ya kundi;[k] nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova." ' "[l]

6 "Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Kwa sababu ulipiga makofi[m] na kupiga vishindo kwa miguu, nawe uliendelea

SURA 24
a Eze 12:9; Eze 37:18
b Zb 74:7; Zb 79:1; Yer 7:14; Omb 1:10; Omb 2:7; Eze 9:7
c Zb 96:6
d Zb 27:4; Zb 84:1
e 2Nya 36:17; Yer 6:11; Yer 9:21; Eze 23:25
f Mik 3:7
g Yer 16:7; Eze 24:17
h Ayu 27:15; Zb 78:64
i Law 26:39; Eze 4:17; Eze 33:10
j Isa 59:11
k Isa 8:18; Isa 20:3; Eze 4:3
l Isa 46:10
m Zb 9:16; Yer 17:15; Eze 25:5
n Eze 24:16
o Kum 28:32; Yer 11:22

Safu ya 2
a Eze 33:21
b Zb 51:15
c Eze 3:26; Eze 33:22; Lu 1:20
d Eze 12:3
e Eze 6:13

SURA 25
f Mwa 19:38; Yer 49:1; Amo 1:13; Sef 2:9
g Met 17:5; Met 24:17; Eze 26:2; Eze 35:2; Eze 35:12
h Ayu 1:3; Eze 25:10
i Law 26:16; Kum 28:33
j 2Sa 12:26; Eze 21:20
k Isa 17:2; Isa 32:14; Sef 2:14
l Isa 37:20; Eze 26:6
m Ayu 27:23; Omb 2:15

kushangilia kwa dhihaka zote
ulizokuwa nazo katika nafsi
yako juu ya nchi ya Israeli,[a]
7 kwa hiyo tazama mimi hapa;
nimekunyooshea mkono wa-
ngu,[b] nami nitakutoa uporwe
na mataifa; nami nitakukatilia
mbali kutoka katikati ya viku-
ndi vya watu na kukuharibu
kutoka katika nchi hizi.[c] Nita-
kuangamiza wewe,[d] nawe uta-
lazimika kujua kwamba mimi
ni Yehova.'

8 "Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova amesema hivi, 'Kwa
sababu Moabu[e] na Seiri[f] wa-
mesema: "Tazama! Nyumba ya
Yuda ni kama mataifa mengi-
ne yote,"[g] **9** kwa hiyo tazama,
ninafungua mteremko wa Mo-
abu katika majiji, katika majiji
yake hadi kwenye mipaka yake,
pambo la nchi hiyo, Beth-yeshi-
mothi,[h] Baal-meoni,[i] Kiriathai-
mu,[j] **10** kwa Watu wa Masha-
riki,[k] pamoja na wana wa Amo-
ni;[l] nami nitaifanya kuwa kitu
cha kumilikiwa, ili isikumbu-
kwe,[m] yaani, wana wa Amoni,
katikati ya mataifa. **11** Nami
nitafanya matendo ya huku-
mu katika Moabu;[n] nao watala-
zimika kujua kwamba mimi ni
Yehova.'[o]

12 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi,
'Kwa sababu Edomu ameten-
da kwa kulipiza kisasi juu
ya nyumba ya Yuda nao wali-
endelea kufanya kosa kwa ka-
diri kubwa na kujilipizia kisasi
juu yao,[p] **13** kwa hiyo Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova ame-
sema hivi: "Pia nitaunyoosha
mkono wangu juu ya Edomu[q]
na kukatilia mbali kutoka kwa-
ke mwanadamu na mnyama
wa kufugwa,[r] nami nitapafa-
nya kuwa ukiwa kutoka Tema-
ni,[a] mpaka Dedani.[b] Wataangu-
ka kwa upanga. **14** 'Nami ni-
taleta kisasi changu juu ya Edo-
mu kwa mkono wa watu wangu
Israeli;[c] nao watafanya katika
Edomu kulingana na hasira ya-
ngu na kulingana na ghadhabu
yangu; nao watalazimika kujua
kisasi changu ni nini,'[d] asema
Bwana Mwenye Enzi Kuu Yeho-
va."'

15 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi,
'Kwa sababu Wafilisti wameten-
da kwa kulipiza kisasi[e] nao
waliendelea kujilipizia kisasi
wenyewe wakiwa na kisasi che-
nye dhihaka katika nafsi, ili ku-
sababisha uharibifu,[f] wakiwa
na uadui unaodumu mpaka wa-
kati usio na kipimo,[g] **16** kwa
hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova amesema hivi: "Tazama,
ninaunyoosha mkono wa-
ngu juu ya Wafilisti,[h] nami ni-
tawakatilia mbali Wakerethi[i]
na kuiangamiza pwani ya baha-
ri inayobaki.[j] **17** Nami nitafa-
nya katikati yao matendo ma-
kubwa ya kisasi, kwa makaripio
yenye ghadhabu;[k] nao watala-
zimika kujua kwamba mimi ni
Yehova nitakapoleta kisasi cha-
ngu juu yao."'"[l]

26 Na ikawa kwamba kati-
ka mwaka wa kumi na
moja, katika siku ya kwanza
ya mwezi, neno la Yehova lili-
nijia, na kusema: **2** "Mwa-
na wa binadamu, kwa saba-
bu Tiro[m] amesema juu ya Ye-
rusalemu,[n] 'Aha! Amevunjwa,[o]
milango ya vikundi vya watu![p]
Hakika mwelekeo wa ma-
mbo utageuka uwe kwangu.
Nitajazwa—ameharibiwa,'[q]

SURA 25

a Ne 4:4
Ayu 31:29
Met 24:17
Oba 12
Sef 2:8
b Eze 35:3
Sef 1:4
c Yer 49:2
Amo 1:14
d Zb 145:20
e Isa 15:1
Yer 48:1
Amo 2:1
f Kum 2:4
g Isa 10:9
Isa 36:18
h Yos 13:20
i Hes 32:38
j Yos 13:19
k Eze 25:4
l Zb 83:7
m Eze 21:32
n Zb 149:7
Yer 9:26
Yer 48:1
o Eze 6:13
p 2Nya 28:17
Zb 137:7
Omb 4:22
Amo 1:11
Oba 10
q Mal 1:4
r Yer 7:20

Safu ya 2

a Yer 49:7
b Yer 49:8
c Isa 11:14
Isa 63:1
Yer 49:2
d Kum 32:35
Zb 58:10
Nah 1:2
Ufu 6:16
e Isa 14:29
Yer 25:20
Yoe 3:4
f 2Nya 28:18
Isa 9:12
Yer 47:1
Amo 1:6
g 1Sa 31:7
2Sa 5:17
h Sef 2:4
i 1Sa 30:14
Sef 2:5
j Yer 47:4
k Eze 5:15
Nah 1:2
l Zb 9:16

SURA 26

m Yos 19:29
n Yoe 3:6
Amo 1:9
o Eze 25:3
p Omb 1:1
q Eze 19:7

3 kwa hiyo Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova amesema
hivi, 'Tazama niko juu yako,
Ee Tiro, nami nitainua mataifa mengi juu yako,[a] kama vile
bahari inavyoinua mawimbi
yake.[b] **4** Na hakika wao wa-
taziharibu kuta za Tiro[c] na
kuibomoa minara yake,[d] nami
nitakwangua mavumbi yake
kutoka kwake na kumfa-
nya kuwa uso ulio wazi na
wenye kung'aa wa mwamba.
5 Atakuwa uwanja wa kukau-
shia nyavu za kukokota[e] kati-
kati ya bahari.'[f]
"'Kwa maana mimi mwe-
nyewe nimesema,' asema Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova,
'naye lazima atakuwa kitu cha
kuporwa na mataifa. **6** Na
miji yake ya kandokando iliyo-
ko shambani—watauawa kwa
upanga, na watu watalazimi-
ka kujua kwamba mimi ni Ye-
hova.'[g]
7 "Kwa maana Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amese-
ma hivi, 'Tazama, juu ya Tiro
ninamleta Nebukadreza mfa-
lme wa Babiloni kutoka ka-
skazini,[h] mfalme wa wafalme,[i]
pamoja na farasi[j] na magari
ya vita[k] na askari wapanda-fa-
rasi na kutaniko,[l] naam, uma-
ti wa watu. **8** Ataua, naam,
kwa upanga, miji yako ya ka-
ndokando iliyoko shambani,
naye atajenga ukuta wa kuku-
zingira na kujenga juu yako
boma la kuzingira[m] na kuinua
juu yako ngao kubwa; **9** na
shambulio la mtambo wake
wa kushambulia atalielekeza juu ya kuta zako, naye ata-
ibomoa minara yako, kwa pa-
nga zake. **10** Kwa sababu ya
umati unaosukasuka wa fara-
si zake mavumbi yao yataku-
funika.[a] Kwa sababu ya sau-
ti ya askari wapanda-farasi
na gurudumu na gari la vita
kuta zako zitatikisika, ataka-
poingia katika malango yako,
kama ilivyo nyakati za kui-
ngia katika jiji lililofunguliwa
kwa matundu yaliyotobolewa.
11 Kwa kwato za farasi zake
atakanyaga-kanyaga barabara
zako zote.[b] Watu wako atawa-
ua, naam, kwa upanga, nazo
nguzo zako zenye nguvu zitaa-
nguka chini. **12** Nao hakika
watateka nyara mali[c] zako na
kupora mali zako za mauzo,[d]
na kubomoa kuta zako, nazo
nyumba zako zenye kutamani-
ka watazibomoa. Nao wataweka mawe yako na mbao zako
na mavumbi yako katikati ya
maji.'
13 "'Nami nitafanya kele-
le za kuimba kwako zikome,[e]
na sauti ya vinubi vyako hai-
tasikiwa tena.[f] **14** Nami ni-
takufanya kuwa uso ulio wazi
na wenye kung'aa, wa mwa-
mba.[g] Utakuwa uwanja wa ku-
kaushia nyavu za kukokota.[h]
Wewe hutajengwa tena ka-
mwe; kwa maana mimi mwe-
nyewe, Yehova, nimesema,'
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova.[i]
15 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amemwambia
Tiro hivi, 'Inapotokea sau-
ti ya kuanguka kwako, wa-
kati ambapo aliyetiwa maje-
raha ya kufisha atakapougua,
wakati ambapo kutakuwapo
mauaji yenye machinjo katika-
ti yako, je, visiwa havitatikisi-
ka?[j] **16** Nao wakuu wote wa
bahari hakika watashuka ku-

SURA 26
a Zb 82:8
b Yer 51:42
c Isa 23:11
Amo 1:10
d Zek 9:4
e Eze 26:14
f Eze 27:32
g Zb 9:16
h Yer 25:9
Eze 29:18
i Ezr 7:12
Da 2:37
j Yer 6:23
Hab 1:8
k Yer 4:13
l Eze 23:24
m 2Sa 20:15
Eze 21:22

Safu ya 2
a Yer 47:3
Eze 26:4
b Isa 5:28
Hab 1:8
c Eze 27:33
1Ti 6:17
d Ne 13:16
Eze 27:33
Eze 28:5
Eze 28:18
Zek 9:3
e Isa 14:11
f Isa 23:16
Isa 24:8
Ufu 18:22
g Eze 26:4
h Eze 26:5
i Isa 14:27
j Yer 49:21
Eze 27:28
Eze 31:16

toka katika viti vyao vya ufalme[a] na kuvua makoti yao yasiyo na mikono, nao watayavua mavazi yao wenyewe yenye mapambo. Watavaa mavazi ya kutetemeka. Wataketi chini,[b] nao hakika watatetemeka kila pindi[c] na kukukazia macho kwa mshangao. **17** Nao wataimba wimbo wa huzuni juu yako[d] na kukuambia:

"'"Lo! Jinsi umeangamia, wewe uliyekuwa ukikaliwa kutoka baharini,[e] wewe jiji lililosifiwa, uliyekuwa mwenye nguvu katika bahari,[f] yeye na wale wanaokaa ndani yake, wale waliowatia wakaaji wote wa dunia woga wao! **18** Sasa visiwa vitatetemeka katika siku ya kuanguka kwako. Na visiwa vilivyomo baharini vitaingiwa na wasiwasi kwa sababu ya kuondoka kwako."'[g]

19 "Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Nitakapokufanya wewe uwe jiji lililoharibiwa, kama majiji ambayo kwa kweli hayakaliwi, nitakapoleta juu yako kilindi cha maji, na maji mengi yawe yamekufunika,[h] **20** pia nitakushusha chini pamoja na wale wanaoshuka kuingia shimoni kwa watu wa zamani za kale,[i] nami nitakufanya ukae katika nchi ya chini zaidi,[j] kama mahali palipoharibiwa kwa muda mrefu, pamoja na wale wanaoshuka kuingia shimoni,[k] ili usipate kukaliwa; nami nitaweka pambo katika nchi ya wale walio hai.[l]

21 "'Nitakufanya kuwa vitisho vya ghafula,[m] nawe hutakuwapo; nawe utatafutwa,[n] lakini hutapatikana tena kamwe mpaka wakati usio na kipimo,'[o] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

27 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, mfanyie Tiro wimbo wa huzuni,[a] **3** nawe utamwambia Tiro,

"'Wewe unayekaa katika malango ya bahari,[b] mwanamke mfanya-biashara wa vikundi vya watu wa visiwa vingi,[c] Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Ee Tiro, wewe mwenyewe umesema, 'Mimi ni mkamilifu wa uzuri.'[d] **4** Maeneo yako yamo katika moyo wa bahari.[e] Wajenzi wako mwenyewe wameukamilisha uzuri wako.[f] **5** Walikutengenezea kutokana na miberoshi kutoka Senir[g] mbao zote. Waliuchukua mwerezi kutoka Lebanoni[h] na kufanya mlingoti juu yako. **6** Waliyafanya makasia yako kutokana na miti mikubwa sana ya Bashani. Waliifanya omo yako kwa pembe za tembo katika mbao za mvinje, kutoka katika visiwa vya Kitimu.[i] **7** Mtando wako wa nguo ulikuwa kitani cha rangi mbalimbali kutoka Misri,[j] ili kuwa tanga yako. Uzi wa bluu[k] na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau[l] kutoka katika visiwa vya Elisha[m] ndivyo vilivyofunika sitaha yako.

8 "'"Wakaaji wa Sidoni[n] na Arvadi[o] wenyewe wakawa wapiga-makasia wako. Watu wako wenye ustadi,[p] Ee Tiro, walikuwa ndani yako; walikuwa mabaharia[q] wako. **9** Hata wanaume wazee wa Gebali[r] na watu wake wenye ustadi

SURA 26
a 1Sa 2:7
Isa 23:8
Yon 3:6
b Isa 3:26
c Kut 15:15
Eze 27:35
Eze 32:10
d Eze 27:32
e Amo 1:9
Ufu 18:10
f Isa 23:4
Eze 28:2
g Isa 23:5
Eze 27:32
h Isa 8:7
Eze 27:34
Da 9:26
i Isa 38:18
j Kum 32:22
Zb 88:6
Eze 32:18
k Zb 143:7
Eze 28:8
Lu 10:15
l Zb 27:13
Eze 32:23
m Eze 27:36
n Zb 37:10
Zb 37:36
o Eze 28:19

Safu ya 2

SURA 27
a Eze 26:17
b Eze 28:2
c Isa 23:8
d Met 27:2
Isa 23:9
Eze 28:12
e Eze 26:5
f Eze 26:12
g Kum 3:9
1Nya 5:23
Wim 4:8
h 1Fa 5:6
i Mwa 10:4
Isa 23:1
Yer 2:10
j Met 7:16
k Kut 25:4
l Yer 10:9
m 1Nya 1:7
n Yos 11:8
o Mwa 10:18
p 2Nya 2:14
q 1Fa 9:27
r Yos 13:5
Zb 83:7

walikuwa ndani yako wakiwa
wenye kutia kalafati mipasu-
ko[a] yako. Meli zote za bahari-
ni na wanamaji wake wenye-
we walikuwa ndani yako, ili
kufanya biashara. **10** Waaje-
mi[b] na Waludimu[c] na watu wa
Putu[d]—walikuwa katika jeshi
lako, watu wako wa vita. Wali-
tundika ngao na kofia kwako.[e]
Wao ndio walioisababisha faha-
ri yako. **11** Wana wa Arvadi,[f]
hata jeshi lako, walikuwa juu
ya kuta zako pande zote, na
watu mashujaa ndio waliokuwa
katika minara yako mwenyewe.
Walizitundika ngao zao za mvi-
ringo juu ya kuta zako kuzu-
nguka pande zote.[g] Wao wenye-
we waliukamilisha uzuri wako.
12 "'"Tarshishi[h] alikuwa
mwanabiashara wako kwa sa-
babu ya wingi wa namna zote
za vitu vyenye thamani.[i] Kwa
ajili ya fedha yake, chuma, bati
na risasi, maghala yake yalito-
lewa.[j] **13** Yavani,[k] Tubali[l] na
Mesheki[m] walikuwa wafanya-
biashara wako. Vitu vyako vya
biashara vilitolewa kwa ajili
ya nafsi za wanadamu[n] na vitu
vya shaba. **14** Kutoka katika
nyumba ya Togarma[o] kuliku-
wa na farasi na farasi wa vita
na nyumbu, ambao kwa ajili
yao maghala yako yalitolewa.
15 Wana wa Dedani[p] waliku-
wa wafanya-biashara wako; vi-
siwa vingi vilikuwa wanabia-
shara uliowaajiri; wamekuli-
pa pembe za tembo[q] na mpi-
ngo kama zawadi. **16** Edomu
alikuwa mwanabiashara wako
kwa sababu ya wingi wa kazi
zako. Maghala yako yalitolewa
kwa ajili ya feruzi,[r] sufu iliyoti-
wa rangi ya zambarau na vita-
mbaa vya rangi mbalimbali na
kitambaa bora na marijani na
zabarijadi.
17 "'"Yuda na nchi ya Isra-
eli walikuwa wafanya-biasha-
ra wako. Vitu vyako vya bi-
ashara vilitolewa[a] kwa ajili ya
ngano[b] ya Minithi[c] na vyakula
vya pekee na asali[d] na mafuta
na zeri.[e]
18 "'"Damasko[f] alikuwa mwa-
nabiashara wako katika wingi
wa kazi zako, kwa sababu ya
wingi wa vitu vyako vyote vye-
nye thamani, pamoja na divai[g]
ya Helboni na sufu ya ra-
ngi ya kijivu. **19** Vedani na
Yavani kutoka Uzali—walitoa
kwa ajili ya maghala yako. Chu-
ma katika kazi ya kufua madi-
ni, kida na kane[h]—vilikuwa kwa
ajili ya vitu vyako vya biashara.
20 Dedani[i] alikuwa mfanya-bia-
shara wako katika mavazi ya vi-
tambaa vilivyofumwa vya ku-
pandia farasi. **21** Waarabu[j] na
wakuu wote wa Kedari[k] wenye-
we walikuwa wanabiashara
uliowaajiri. Katika wana-ko-
ndoo na kondoo-dume na mbuzi-
dume[l]—walikuwa wanabiashara
katika hao. **22** Wafanya-bia-
shara wa Sheba[m] na Raama[n] we-
nyewe walikuwa wafanya-biasha-
ra wako; kwa ajili ya namna zote
za manukato yaliyo bora zaidi na
kwa ajili ya namna zote za mawe
ya thamani na dhahabu, magha-
la yako yalitolewa.[o] **23** Harani[p]
na Kane na Edeni,[q] wafanya-bi-
ashara wa Sheba,[r] Asihuru[s]
na Kilmadi walikuwa wafanya-
biashara wako. **24** Walikuwa
wafanya-biashara wako kati-
ka mavazi ya fahari, katika mi-
tandio ya kitambaa cha bluu
na kitambaa cha rangi mbali-
mbali na katika mazulia ya

SURA 27

a 1Fa 5:18
Eze 27:27
b Eze 38:5
c Mwa 10:13
d 1Nya 1:8
Yer 46:9
Eze 30:5
Nah 3:9
e Eze 38:5
f Mwa 10:18
g Wim 4:4
h Mwa 10:4
1Fa 10:22
Isa 2:16
Yon 1:3
i 2Nya 9:21
2Nya 20:36
Zb 72:10
j Yer 10:9
k Mwa 10:2
Isa 66:19
l 1Nya 1:5
m Eze 32:26
n Yoe 3:6
Ufu 18:13
o Mwa 10:3
1Nya 1:6
Eze 38:6
p Mwa 10:7
1Nya 1:9
Yer 25:23
q 1Fa 10:22
Ufu 18:12
r Eze 28:13

Safu ya 2

a 1Fa 5:9
2Nya 2:10
Ezr 3:7
Mdo 12:20
b Kum 8:8
c Amu 11:33
d Mwa 43:11
e Yer 8:22
f Isa 7:8
g Mhu 10:19
h Wim 4:14
i Mwa 25:3
j Yer 25:24
k Mwa 25:13
1Nya 1:29
Wim 1:5
Isa 60:7
l 2Nya 17:11
m 1Fa 10:1
2Nya 9:1
Zb 72:10
n Mwa 10:7
1Nya 1:9
o 1Fa 10:2
Isa 60:6
p Mwa 11:31
q 2Fa 19:12
Isa 37:12
Amo 1:5
r Mwa 25:3
Ayu 6:19
s Mwa 10:22
1Nya 1:17

nguo za rangi mbili, katika kamba zilizosokotwa na kufanywa kuwa thabiti, katika kituo chako cha kufanyia biashara.

25 “‘“Meli za Tarshishi[a] zilikuwa misafara yako ya vitu vyako vya biashara, hivi kwamba unajazwa na kuwa na utukufu sana katika moyo wa bahari kuu.[b]

26 “‘“Wale wanaokupigia makasia wamekuleta katika maji makuu.[c] Upepo wa mashariki umekuvunja katika moyo wa bahari kuu.[d] **27** Vitu vyako vyenye thamani na maghala yako,[e] vitu vyako vya biashara,[f] wanamaji wako na mabaharia[g] wako, wenye kutia kalafati mipasuko[h] yako na wale wanaofanya biashara na watu wako wote wa vita,[i] walio ndani yako na katika kutaniko lako lote, walio katikati yako, —wataanguka katika moyo wa bahari kuu katika siku ya kuanguka kwako.[j]

28 “‘“Nchi iliyo wazi itatikisika itakaposikia sauti ya kilio cha mabaharia wako.[k] **29** Na wale wote wanaotumia kasia, wanamaji, mabaharia wote wa baharini, hakika watashuka kutoka katika meli zao; watasimama juu ya nchi.[l] **30** Nao hakika watajiacha wasikiwe juu yako kwa sauti yao nao watapaaza kilio kwa uchungu.[m] Nao watatia mavumbi juu ya vichwa vyao.[n] Watagaagaa katika majivu.[o] **31** Nao watajitia upara kwa ajili yako,[p] na kujifunga nguo za magunia[q] na kukulilia wewe kwa uchungu wa nafsi, kwa kuomboleza kwa uchungu.[r] **32** Nao katika maombolezo yao watakuimbia wimbo wa huzuni,[a]

“‘“‘Ni nani aliye kama Tiro,[b] kama yeye ambaye amenyamazishwa katikati ya bahari?[c] **33** Maghala[d] yako yalipotoka katika bahari kuu,[e] uliwashibisha watu wengi.[f] Kwa wingi wa vitu vyako vyenye thamani na vitu vyako vya biashara uliwatajirisha wafalme wa dunia.[g] **34** Sasa umevunjwa na bahari kuu, katika vilindi vya maji.[h] Navyo vitu vyako vya biashara na kutaniko lako lote,[i] vimeanguka katikati yako. **35** Wakaaji wote wa visiwa[j]—hakika watakukazia macho kwa mshangao, nao wafalme wao wenyewe watalazimika kutetemeka kwa hofu.[k] Nyuso zitaingiwa na wasiwasi.[l] **36** Nao wanabiashara kati ya vikundi vya watu, hakika watapiga mluzi juu yako.[m] Utakuwa vitisho vya ghafula, nawe hutakuwapo tena mpaka wakati usio na kipimo.’”’”[n]

28 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** “Mwana wa binadamu, mwambie kiongozi wa Tiro, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi:

“‘“Kwa sababu moyo wako umekuwa na majivuno,[o] nawe unaendelea kusema, ‘Mimi ni mungu.[p] Katika kiti cha mungu nimejiketisha mwenyewe,[q] katika moyo wa bahari kuu,’[r] wakati ambapo wewe ni mtu wa udongo,[s] wala si mungu,[t] nawe unaendelea kuufanya moyo wako kama moyo wa mungu— **3** tazama! wewe una hekima kuliko Danieli.[u] Hakuna siri ambazo zimelingana na

SURA 27
a 1Fa 10:22; Isa 2:16; Isa 23:14; Isa 60:9
b Eze 27:4; Yon 2:3
c Eze 27:8
d Zb 48:7
e Eze 27:14
f Eze 27:13
g Eze 27:8
h Eze 27:9
i Eze 27:11
j Met 11:4; Eze 26:14
k Eze 26:15; Ufu 18:17
l Eze 26:16
m Isa 23:1; Eze 26:17; Ufu 18:9; Ufu 18:11
n Ne 9:1; Ayu 2:12; Ufu 18:19
o Est 4:1; Yer 6:26
p Isa 15:2; Yer 16:6; Mik 1:16
q Est 4:3; Isa 22:12; Da 9:3
r Isa 22:4

Safu ya 2
a Eze 26:17; Eze 27:2
b Omb 2:13; Ufu 18:18
c Eze 26:5
d Eze 27:14; Eze 27:16; Ufu 18:19
e Eze 27:26
f Isa 23:3
g Zek 9:3; Ufu 18:3
h Eze 26:19
i Eze 27:27
j Isa 23:6; Eze 26:15
k Eze 28:17; Eze 32:10; Ufu 18:9
l Ufu 18:10
m Yer 18:16; Yer 19:8; Ufu 18:15
n Zb 37:10; Eze 26:14

SURA 28
o Met 16:18; Isa 2:12; Eze 28:5
p Da 11:36; 1Ko 8:5
q Isa 14:13; 2Th 2:4
r Eze 27:4
s Zb 144:3
t Isa 31:3
u Da 2:48

wewe.[a] **4** Kwa hekima yako
na kwa utambuzi wako umeji-
patia mali, nawe unaendelea ku-
pata dhahabu na fedha kati-
ka maghala yako.[b] **5** Kwa wi-
ngi wa hekima yako,[c] kwa
mali zako za mauzo,[d] umefanya
utajiri wako uwe mwingi,[e] nao
moyo wako ukaanza kuwa na
majivuno kwa sababu ya utajiri
wako."'[f]

6 "'Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amese-
ma hivi: "Kwa sababu unau-
fanya moyo wako kama moyo
wa mungu,[g] **7** kwa hiyo ta-
zama, ninaleta juu yako wa-
geni,[h] waonevu wa mataifa,[i]
nao hakika watachomoa pa-
nga zao juu ya uzuri wa heki-
ma yako na kutia unajisi fahari
yako inayong'aa.[j] **8** Watak-
ushusha chini mpaka shimoni,[k]
nawe utakufa kifo cha mtu ali-
yeuawa katika moyo wa baha-
ri kuu.[l] **9** Je, kwa hakika uta-
sema, 'Mimi ni mungu,' mbele
yake yeye anayekuua,[m] wakati
ambapo wewe ni mtu wa udo-
ngo tu, wala si mungu,[n] mkono-
ni mwa wale wanaokutia una-
jisi?"'

10 "'Kwa mkono wa wageni
utakufa vifo vya watu ambao
hawajatahiriwa,[o] kwa maana
mimi mwenyewe nimesema,'
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova."

11 Nalo neno la Yehova li-
kaendelea kunijia, na kusema:
12 "Mwana wa binadamu, mfa-
nyie mfalme wa Tiro wimbo
wa huzuni,[p] nawe umwambie,
'Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova amesema hivi:

"'"Unafunga kielelezo kwa
muhuri, kinachojaa hekima[q]
na kikamilifu katika uzuri.[r]

SURA 28

a Zek 9:2
b Kum 8:17
Met 23:4
Zek 9:3
c Zek 9:2
d Eze 26:12
Eze 28:18
e Isa 23:3
Eze 27:12
f Met 11:28
Met 18:11
g Lu 14:11
h Eze 30:11
i Kum 28:50
j Isa 23:9
k Ayu 17:16
l Eze 27:26
m Zb 82:7
n Isa 31:3
o Yer 9:26
p Eze 26:17
q Met 21:30
Isa 10:13
Yer 9:23
Eze 28:3
Zek 9:2
r Eze 27:3

Safu ya 2

a Eze 31:8
b Mwa 2:12
c Eze 27:16
d Isa 14:13
e 1Fa 5:1
f Yoe 3:4
Amo 1:9
g 1Fa 10:11
2Nya 9:21
Eze 27:12
Yoe 3:5
h Yoe 3:6
i Isa 23:9
Yer 25:17
Yer 25:22
Yer 47:4
Yoe 3:8
j Met 11:2
Met 16:18
Eze 27:3
k Isa 14:14
Yer 8:9
l Ayu 40:11
Zb 73:18
Zb 147:6
Isa 14:15
m Eze 26:3
n Eze 28:2
o Eze 28:16
p Amo 1:10

13 Ulikuwa katika Edeni, bu-
stani ya Mungu.[a] Kila jiwe la
thamani lilikuwa kifuniko
chako, zabarijadi, topazi na ya-
spi; krisolito, shohamu[b] na ya-
shefi; yakuti, feruzi[c] na zuma-
ridi; nao ufundi wa viwekeo
na wa vitundu vyako ulikuwa
wa dhahabu ndani yako. Vili-
tayarishwa katika siku ya kuu-
mbwa kwako. **14** Wewe ndi-
ye kerubi aliyetiwa mafuta
anayefunika, nami nimeku-
weka wewe. Ulikuwa katika
mlima mtakatifu wa Mungu.[d]
Ulitembea katikati ya mawe
yenye moto. **15** Hukuwa na
kosa katika njia zako tangu
siku ya kuumbwa[e] kwako mpa-
ka ukosefu wa uadilifu ulipoo-
nekana ndani yako.[f]

16 "'"Kwa sababu ya wingi
wa mali zako za mauzo[g] walikuj-
aza jeuri katikati yako, nawe
ukaanza kutenda dhambi.[h]
Nami nitakufukuza kama uli-
ye najisi kutoka katika mlima
wa Mungu, nami nitakuharibu
wewe,[i] Ee kerubi unayefunika,
kutoka katikati ya mawe yenye
moto.

17 "'"Moyo wako ulikuwa
na majivuno kwa sababu ya
urembo wako.[j] Uliiharibu heki-
ma yako kwa sababu ya fa-
hari yako inayong'aa.[k] Nitaku-
tupa chini.[l] Nitakuweka mbele
ya wafalme, ili wakutazame.[m]

18 "'"Kwa sababu ya wingi
wa makosa yako,[n] kwa saba-
bu ya ukosefu wa haki wa mali
zako za mauzo,[o] umepatia una-
jisi patakatifu pako. Nami ni-
tatokeza moto kutoka kati-
kati yako. Huo ndio utakaoku-
teketeza.[p] Nami nitakufanya
kuwa majivu juu ya dunia mbe-
le ya macho ya wale wanaokuo-

na.[a] **19** Nao wale wote wanaokujua wewe katikati ya vikundi vya watu, hakika watakukazia macho kwa mshangao.[b] Utakuwa vitisho vya ghafula, nawe hutaendelea kuwapo tena mpaka wakati usio na kipimo."'"[c]

20 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **21** "Mwana wa binadamu, elekeza uso wako Sidoni,[d] na utoe unabii juu yake. **22** Nawe utasema, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Tazama, niko juu yako,[e] Ee Sidoni, nami hakika nitatukuzwa katikati yako;[f] nao watu watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapofanya matendo ya hukumu[g] ndani yake nami kwa kweli nitakaswe ndani yake.[h] **23** Nami nitatuma tauni ndani yake na damu katika barabara zake.[i] Na aliyeuawa ataanguka katikati yake kwa upanga juu yake kila upande;[j] nao watu watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.[k] **24** Na katika nyumba ya Israeli hakutakuwa tena na mchongoma hatari[l] au mwiba wenye kuumiza kutoka kwa wote hao wanaowazunguka pande zote, wale wanaowatendea kwa dhihaka; na watu watalazimika kujua kwamba mimi ni Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."'

25 "'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Nitakapokusanya pamoja nyumba ya Israeli kutoka kwa vikundi vya watu ambao kati yao wametawanyika,[m] mimi pia nitatakaswa kati yao machoni pa mataifa.[n] Nao hakika watakaa kwenye nchi[o] yao niliyompa mtumishi wangu, Yakobo.[a] **26** Nao kwa kweli watakaa juu yake kwa usalama[b] na kujenga nyumba[c] na kupanda mashamba ya mizabibu,[d] nao watakaa kwa usalama[e] ninapofanya matendo ya hukumu juu ya wale wote wanaowatendea kwa dhihaka kuwazunguka pande zote;[f] nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova Mungu wao."'"

29 Katika mwaka wa kumi, mwezi wa kumi, siku ya kumi na mbili ya mwezi huo, neno la Yehova lilinijia, na kusema: **2** "Mwana wa binadamu, elekeza uso wako kwa Farao mfalme wa Misri[g] na utoe unabii juu yake na juu ya Misri yote.[h] **3** Ongea, nawe useme, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Tazama niko juu yako, Ee Farao, mfalme wa Misri,[i] yule mnyama mkubwa wa baharini[j] anayelala akiwa amejinyoosha katikati ya mifereji yake ya Nile,[k] ambaye amesema, 'Mto wangu wa Nile ni wangu, na mimi—mimi nimeufanya kwa ajili yangu mwenyewe.'[l] **4** Nami nitaweka kulabu katika mataya yako[m] na kufanya samaki wa mifereji yako ya Nile washikamane na magamba yako. Nami nitakutoa kutoka katikati ya mifereji yako ya Nile na samaki wote wa mifereji yako ya Nile wanaoshikamana na magamba yako. **5** Nami nitakuacha nyikani, wewe na samaki wote wa mifereji yako ya Nile.[n] Utaanguka juu ya uso wa nchi.[o] Hutaokotwa wala kukusanywa pamoja. Nitakutoa uwe chakula

SURA 28
a Mal 4:3
b Eze 27:35
c Eze 26:21
Eze 27:36
d Isa 23:4
Yer 25:22
Eze 32:30
e Eze 26:3
f Kut 9:16
Eze 39:13
g Zb 9:16
h Eze 20:41
Eze 36:23
Eze 38:23
i Eze 38:22
j Yer 25:33
k Eze 26:6
l Hes 33:55
Yos 23:13
m Kum 30:3
Zb 106:47
Isa 11:12
Yer 30:18
Ho 1:11
n Isa 5:16
o Yer 23:8
Eze 36:28

Safu ya 2
a Mwa 28:13
b Yer 23:6
Ho 2:18
c Isa 65:21
Yer 31:4
d Yer 31:5
Eze 36:36
Amo 9:14
e Isa 32:18
Eze 38:11
f Yer 30:16

SURA 29
g Yer 44:30
h Isa 19:1
Yer 25:19
Yer 43:11
Eze 31:2
i Yer 46:25
Eze 31:18
j Zb 74:13
Isa 27:1
Isa 30:7
Isa 51:9
k Eze 32:2
l Isa 10:13
Eze 29:9
m 2Fa 19:28
Isa 37:29
Eze 38:4
n Kut 7:21
o Yer 16:4
Yer 25:33

kwa wanyama-mwitu wa dunia
na kwa viumbe vinavyoruka
vya mbinguni.[a] **6** Na wakaa-
ji wote wa Misri watalazimi-
ka kujua kwamba mimi ni Ye-
hova,[b] kwa sababu walikuwa,
kama kitegemeo, utete kwa
nyumba ya Israeli.[c] **7** Wali-
pokushika mkono, ulipondwa,[d]
nawe ulifanya bega lao lote li-
pasuke. Na walipojitegemeza
juu yako, ulivunjika,[e] nawe uli-
fanya viuno vyao vyote vitete-
meke."[f]

8 "'Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amesema
hivi: "Tazama, ninaleta upa-
nga juu yako,[g] nami nitakati-
lia mbali kutoka kwako mtu
wa udongo na mnyama wa ku-
fugwa.[h] **9** Nayo nchi ya Misri
itakuwa mahame yenye ukiwa
na mahali palipoharibiwa;[i] nao
watalazimika kujua kwamba
mimi ni Yehova, kwa sababu
amesema, 'Mto Nile ni wangu,
na mimi mwenyewe nimeufa-
nya.'[j] **10** Kwa hiyo tazama,
niko juu yako na juu ya mife-
reji yako ya Nile,[k] nami nitai-
fanya nchi ya Misri iwe maha-
li palipoharibiwa, ukavu, ma-
hame yaliyotiwa ukiwa,[l] kuto-
ka Migdoli[m] hadi Sewene[n] na
hadi mpaka wa Ethiopia.
11 Mguu wa mtu wa udongo
hautapita katikati yake,[o] wala
mguu wa mnyama wa kufu-
gwa hautapita katikati yake,[p]
na kwa miaka 40 haitakaliwa.[q]
12 Nami nitaifanya nchi ya
Misri iwe mahame yenye ukiwa
katikati ya nchi zilizofa-
nywa ukiwa;[r] na majiji yake
yatakuwa mahame yenye ukiwa
katikati ya majiji yaliyoha-
ribiwa kwa miaka 40;[s] nami ni-
tawatawanya Wamisri katika-
ti ya mataifa na kuwatapanya
katika nchi mbalimbali."[a]

13 "'Kwa maana Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova ame-
sema hivi: "Mwishoni mwa mi-
aka 40[b] nitawakusanya Wami-
sri pamoja kutoka kati ya viku-
ndi vya watu ambamo watuku-
wa wametawanywa,[c] **14** nami
nitarudisha kundi la mateka
ya Wamisri; nami nitawarudi-
sha katika nchi ya Pathro-
si,[d] katika nchi ya asili yao,
nao huko watakuwa ufalme
wa hali ya chini. **15** Itaku-
wa chini kuliko zile falme nyi-
ngine, nayo haitajiinua yenye-
we tena juu ya mataifa mengi-
ne,[e] nami nitawafanya kuwa
wachache sana ili wasiweze
kuyatiisha mataifa mengine.[f]
16 Haitakuwa tena uhakika
wa nyumba ya Israeli,[g] ku-
fanya kosa likumbukwe kwa
wao kugeuka na kuwafuati-
lia.[h] Nao watalazimika kujua
kwamba mimi ndiye Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova."'"

17 Sasa ikawa kwamba kati-
ka mwaka wa 27, mwezi wa kwa-
nza, siku ya kwanza ya mwe-
zi huo, neno la Yehova likani-
jia, na kusema: **18** "Mwana
wa binadamu, Nebukadreza
mwenyewe,[i] mfalme wa Ba-
biloni, alitumikisha jeshi lake
utumishi mkubwa juu ya Tiro.[j]
Kila kichwa kilitiwa upara,
na kila bega lilikwaruzwa.[k] La-
kini kuhusu malipo,[l] hapaku-
wa na malipo yoyote kwa aji-
li yake na jeshi lake kutoka
Tiro kwa ajili ya utumishi alio-
kuwa amefanya juu yake.

19 "Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amese-
ma hivi, 'Tazama, ninampa Ne-

SURA 29

a 1Sa 17:44
Yer 7:33
Yer 34:20
Eze 32:4
Eze 39:4
Ufu 19:18
b Kut 9:14
Ro 9:17
c 2Fa 18:21
Isa 30:3
Isa 31:3
Isa 36:6
Eze 17:17
d Yer 37:7
e Zb 118:8
Zb 146:3
Yer 17:5
f Zb 69:23
Eze 21:6
g Yer 46:14
Eze 30:4
h Kut 12:12
Yer 7:20
i Yer 43:12
Eze 30:7
j Eze 29:3
k Kut 7:19
l Isa 19:7
Eze 30:12
m Kut 14:2
Yer 44:1
Yer 46:14
n Eze 30:6
o Eze 31:12
p Eze 32:13
q 2Nya 36:21
r Eze 30:7
s Yer 46:19

Safu ya 2

a Eze 30:23
b Eze 29:11
c Isa 19:22
Yer 46:26
d Mwa 10:14
1Nya 1:12
Eze 30:14
e Eze 30:13
f Eze 32:2
Da 11:42
g Isa 30:2
Isa 36:4
Yer 2:18
Yer 37:5
Omb 4:17
Ho 7:11
h Zb 79:8
Isa 64:9
i Yer 25:9
Yer 27:6
j Eze 26:7
k Eze 26:17
l Isa 62:11

bukadreza mfalme wa Babiloni nchi ya Misri,[a] naye atauchukua utajiri wake na kuteka nyara kubwa kutokana nayo[b] na kuipora kwa wingi sana; nayo itakuwa malipo kwa ajili ya jeshi lake.'

20 "'Nami nimempa nchi ya Misri iwe malipo yake kwa ajili ya utumishi ambao alifanya juu yake, kwa sababu walitenda kwa ajili yangu,'[c] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

21 "Katika siku hiyo nitafanya pembe ichipuke kwa ajili ya nyumba ya Israeli,[d] nami nitakupa sababu ya kufungua kinywa katikati yao;[e] nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova."

30 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** "Mwana wa binadamu, toa unabii, nawe useme,[f] 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Pigeni mayowe, 'Ole wa siku ile!'[g] **3** kwa maana siku iko karibu, naam, siku ya Yehova iko karibu.[h] Siku ya mawingu,[i] itakuwa wakati uliowekwa wa mataifa.[j] **4** Na hakika upanga utaingia Misri,[k] na maumivu makali yatatukia Ethiopia wakati ambapo mtu ataanguka akiwa ameuawa katika Misri nao kwa kweli wachukue mali yake nayo misingi yake kwa kweli ibomolewe.[l] **5** Ethiopia[m] na Putu[n]na Ludi na jamii yote iliyochangamana[o] na Kubu na wana wa nchi ya agano—pamoja nao wataanguka kwa upanga."'[p]

6 "Yehova amesema hivi, 'Wanaounga mkono Misri lazima waanguke pia, na fahari ya nguvu zake lazima ishuke chini.'[a]

"'Kutoka Migdoli[b] mpaka Sewene[c] wataanguka ndani yake kwa upanga,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **7** 'Lazima pia wafanywe kuwa ukiwa katikati ya nchi zilizofanywa ukiwa, na majiji yake yatakuwa katikati kabisa ya majiji yaliyoharibiwa.[d] **8** Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapowasha moto katika Misri na wasaidizi wake wote kwa kweli wavunjwe.[e] **9** Katika siku hiyo wajumbe watatoka mbele zangu katika meli, ili kuifanya Ethiopia yenye kujitumaini ianze kutetemeka.[f] Na maumivu makali yatatukia kati yao katika siku ya Misri, kwa maana, tazama! lazima ije.'[g]

10 "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Nitaufanya pia umati wa Misri ukome kwa mkono wa Nebukadreza mfalme wa Babiloni.[h] **11** Yeye na watu wake pamoja naye, watu wa mataifa wenye kuonea,[i] wanaletwa ndani ili kuiharibu nchi. Nao watachomoa panga zao juu ya Misri na kuijaza nchi kwa waliouawa.[j] **12** Nami nitaifanya mifereji ya Nile[k] iwe nchi kavu na kuiuza nchi mkononi mwa watu wabaya,[l] nami nitaifanya nchi na vyote vinavyoijaza ifanywe ukiwa kwa mkono wa wageni.[m] Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema.'[n]

13 "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Nitaangamiza pia sanamu za mavi[o] na kufanya miungu isiyo na

SURA 29
a Yer 43:10
Yer 43:12
b Eze 32:12
c Eze 30:9
Eze 30:10
d 1Sa 2:10
Zb 132:17
Yer 23:5
Lu 1:69
e Zb 51:15
Eze 3:27
Eze 24:27
Lu 21:15

SURA 30
f 2Pe 1:21
g Yer 25:34
h Yoe 2:1
Oba 15
Sef 1:7
i Eze 32:7
Yoe 2:2
j Zb 110:6
Isa 24:21
Zek 14:3
k Isa 19:2
l Isa 19:16
Eze 32:12
m Sef 2:12
n Nah 3:9
o Yer 25:24
Eze 27:10
p Yer 44:27

Safu ya 2
a Isa 20:5
Isa 31:3
Eze 30:18
b Kut 14:2
Yer 44:1
Yer 46:14
c Eze 29:10
d Yer 46:19
Eze 29:12
Eze 32:18
e Eze 30:6
f Isa 20:4
g Isa 55:11
Eze 33:33
h Eze 29:19
Eze 32:11
i Eze 28:7
Hab 1:6
j Isa 34:3
Eze 29:5
k Isa 19:6
Eze 29:3
l Isa 19:4
m Eze 31:12
n Isa 46:10
o Isa 19:1
Yer 43:12
Zek 13:2

thamani ikome katika Nofu,[a]
na hakutakuwa tena na mkuu
kutoka katika nchi ya Misri;
nami hakika nitatia hofu ka-
tika nchi ya Misri.[b] **14** Nami
nitafanya Pathrosi[c] kuwa uki-
wa na kuwasha moto katika So-
ani[d] na kufanya matendo ya
hukumu katika No.[e] **15** Nami ni-
taimwaga ghadhabu yangu[f] juu
ya Sini, ngome ya Misri, na ku-
kutilia mbali umati wa No.[g]
16 Nami nitawasha moto ka-
tika Misri. Hakika Sini itaku-
wa katika maumivu makali, na
No yenyewe itatekwa kwa ku-
tobolewa matundu; na kwa ha-
bari ya Nofu—kutakuwa na
wapinzani wakati wa mchana!
17 Nao vijana wa Oni[h] na Pi-
besethi, wataanguka kwa upa-
nga, na majiji yataenda ute-
kwani. **18** Na katika Tehaf-
nehesi[i] siku itakuwa na giza,
nitakapovunja huko nira za
Misri.[j] Na katika yeye faha-
ri ya nguvu zake kwa kweli
itakomeshwa.[k] Na kwa haba-
ri yake, mawingu yatamfuni-
ka,[l] na miji yake mwenyewe ya
kandokando itaenda utekwa-
ni.[m] **19** Nami nitafanya ma-
tendo ya hukumu katika Mi-
sri;[n] nao watalazimika kujua
kwamba mimi ni Yehova.'"

20 Na ikazidi kuwa kwa-
mba katika mwaka wa kumi
na moja, katika mwezi wa kwa-
nza, siku ya saba ya mwezi huo,
neno la Yehova likanijia, na ku-
sema: **21** "Mwana wa binada-
mu, hakika nitauvunja mkono
wa Farao mfalme wa Misri,[o] na,
tazama! hautafungwa hata ki-
dogo ili kuufanya upone kwa
kutia kitambaa ili kuufunga,[p]
ili uwe na nguvu za kushika
upanga."

SURA 30
a Yer 44:1
Yer 46:14
b Isa 19:16
Yer 46:5
c Mwa 10:14
1Nya 1:12
Yer 44:1
d Hes 13:22
Zb 78:12
e Yer 46:25
f Nah 1:6
g Yer 46:25
h Yer 43:13
i Yer 2:16
j Eze 30:8
k Yer 46:20
Eze 31:18
l Isa 19:1
m Yer 46:19
n Zb 9:16
o Zb 10:15
p Yer 46:11

Safu ya 2
a Yer 46:25
Eze 29:3
b Zb 37:17
c 2Fa 24:7
Yer 46:2
d Yer 46:21
e Eze 29:12
f Yer 27:6
g Kum 32:41
Zb 17:13
Eze 32:11
h Yer 51:52
i Kut 7:5
Zb 9:16
Eze 29:12
Eze 29:19
Eze 29:20
j Eze 29:12

SURA 31
k Yer 46:2
Eze 29:2
l Zb 80:10
Isa 37:24
Eze 17:3
m Isa 10:33

22 "Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amesema
hivi, 'Tazama, mimi niko dhi-
di ya Farao mfalme wa Misri,[a]
nami nitaivunja mikono yake,[b]
ule wenye nguvu na ule ulio-
vunjika,[c] nami nitaufanya upa-
nga uanguke kutoka mkononi
mwake.[d] **23** Nami nitawata-
wanya Wamisri kati ya mataifa
na kuwatapanya kati ya nchi
mbalimbali.[e] **24** Nami nitai-
tia nguvu mikono ya mfalme
wa Babiloni[f] na kuutia upa-
nga wangu mkononi mwake,[g]
nami nitaivunja mikono ya Fa-
rao, naye ataugua kwelikweli
mbele yake kama mwenye ma-
jeraha ya kufisha.[h] **25** Nami
nitaitia nguvu mikono ya mfa-
lme wa Babiloni, na mikono
yenyewe ya Farao itaanguka;
nao watalazimika kujua kwa-
mba mimi ni Yehova nitaka-
poutia upanga wangu mkononi
mwa mfalme wa Babiloni naye
kwa kweli aunyooshe juu ya
nchi ya Misri.[i] **26** Nami ni-
tawatawanya Wamisri kati ya
mataifa[j] na kuwatapanya kati
ya nchi mbalimbali; nao wata-
lazimika kujua kwamba mimi
ni Yehova.'"

31 Na ikazidi kutukia kwa-
mba katika mwaka wa
kumi na moja, katika mwe-
zi wa tatu, siku ya kwanza ya
mwezi huo, neno la Yehova li-
kanijia, na kusema: **2** "Mwa-
na wa binadamu, mwambie Fa-
rao mfalme wa Misri na umati
wake,[k]

"'Umefanana na nani katika
ukuu wako? **3** Tazama! Mwa-
shuru, mwerezi katika Leba-
noni,[l] wenye matawi ya kupe-
ndeza,[m] wenye kifuniko che-

nye majani mengi kinachotoa
kivuli, na wenye kimo kirefu,[a]
hivi kwamba kilele chake kili-
kuwa kati ya mawingu.[b] **4** Ni
maji yaliyoufanya uwe mku-
bwa;[c] kilindi cha maji kiliufa-
nya urefuke. Pamoja na vijito
vyake kilikuwa kikienda kuzu-
nguka pande zote mahali uli-
popandwa; nacho kiliipeleka
mifereji yake kwenye miti yote
ya shambani. **5** Ndiyo saba-
bu ulikuwa mrefu zaidi kwa
kimo kuliko miti mingine yote
ya shambani.[d]

"'Na matawi yake yalizidi
kuongezeka, na matawi yake
yaliendelea kuwa marefu za-
idi kwa sababu ya maji me-
ngi kwenye mifereji ya maji.[e]
6 Viumbe vyote vinavyoru-
ka vya mbinguni vilifanya vio-
ta[f] vyao kwenye matawi yake,
na wanyama wote wa mwitu-
ni walizaa chini ya matawi
yake,[g] na mataifa yote yenye
hesabu kubwa ya watu yaliku-
wa yakikaa katika kivuli cha-
ke. **7** Nao ukawa wenye ku-
pendeza katika ukuu wake,[h]
katika urefu wa majani yake,
kwa maana mizizi yake iliku-
wa juu ya maji mengi. **8** Mi-
erezi mingine haikulingana
nao katika bustani ya Mungu.[i]
Nayo miberoshi, haikufana-
na nao kwa habari ya mata-
wi yake. Na miaramoni yenye-
we haikuwa kama huo katika
matawi yake. Hakuna mti mwi-
ngine wowote katika bustani
ya Mungu uliofanana nao kati-
ka uzuri wake.[j] **9** Niliufanya
kuwa mzuri katika wingi wa
majani yake,[k] na miti mingine
yote ya Edeni iliyokuwa kati-
ka bustani ya Mungu wa kweli
ikawa ikiuonea wivu.'[l]

SURA 31

a Da 4:10

b Eze 17:22

c Eze 17:5

d Zb 37:35

e Da 4:12

f Zb 84:3

g Eze 17:23
Da 4:21

h Da 4:22
Amo 2:9

i Mwa 2:8
Mwa 13:10
Zb 80:10
Eze 28:13

j Zb 37:35

k Da 4:21

l Met 28:22

Safu ya 2

a Mt 23:12

b Yer 50:31
Eze 28:17
Da 4:30

c Eze 30:11
Hab 1:6

d Kum 18:12

e Eze 32:5

f Da 4:14

g Isa 18:6
Eze 29:5
Eze 32:4

h Zb 82:7

i Zb 63:9
Eze 32:18

j Ufu 18:9

10 "Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amesema
hivi, 'Kwa sababu wewe uliku-
wa na kimo kirefu, hivi kwa-
mba huo ukaweka kilele cha-
ke kati ya mawingu[a] na moyo
wake ukainuliwa kwa sababu
ya kimo chake,[b] **11** mimi ni-
tautia pia mkononi mwa mdha-
limu wa mataifa.[c] Hakika ata-
uchukulia hatua. Nitaufukuza
huo kulingana na uovu wake.[d]
12 Na wageni, watu wa mata-
ifa wenye kuonea, wataukata,
na watu watauacha milimani;
na katika mabonde yote maja-
ni yake hakika yataanguka, na
matawi yake yatavunjwa kati-
kati ya sakafu zote za vijito vya
dunia.[e] Na vikundi vyote vya
watu wa dunia watashuka ku-
toka katika kivuli chake na ku-
uacha.[f] **13** Viumbe vyote vi-
navyoruka vya mbinguni vita-
kaa juu ya shina lake lililoa-
nguka, na wanyama wote wa
mwituni hakika watakuwa juu
ya matawi yake;[g] **14** ili wo-
wote kati ya miti iliyonywe-
shwa maji vizuri usipate kuwa
na kimo kirefu, au kuweka vi-
lele vyake kati ya mawingu,
na ili wowote ule unaokunywa
maji usiweze kusimama juu
yake kwa kimo, kwa maana
yote hiyo hakika itatolewa ife,[h]
kwenda kwa nchi iliyo chini,[i]
katikati ya wana wa binadamu,
kwa wale wanaoshuka kuingia
shimoni.'

15 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi,
'Hakika nitasababisha mao-
mbolezo katika siku yake ya
kushuka kuingia katika Kabu-
ri.*[j] Nitakifunika kilindi cha

Eze 31:15* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

maji kwa sababu yake, nipate
kuvizuia vijito vyake na ili yale
maji mengi yazuiliwe; na kwa
sababu yake nitatia giza Leba-
noni, na kwa sababu yake miti
yote ya shambani itazimia.
16 Wakati wa sauti ya kuangu-
ka kwake hakika nitasababi-
sha mataifa yatikisike wakati
nitakapoishusha chini mpaka
katika Kaburi* pamoja na wale
wanaoshuka kuingia shimo-
ni,[a] na katika nchi iliyo chini
miti yote ya Edeni,[b] iliyo bora
na iliyo mizuri kabisa ya Le-
banoni, yote ile inayokunywa
maji, itafarijiwa.[c] **17** Pamoja
naye wao wenyewe pia wame-
shuka mpaka katika Kaburi,*[d]
kwa wale walioiuawa kwa upa-
nga, na wale ambao kama mbe-
gu yake wamekaa katika kivu-
li chake katikati ya mataifa.'[e]
18 "'Umefanana na nani hi-
vyo katika utukufu[f] na ukuu
katikati ya miti ya Edeni?[g] La-
kini hakika utashushwa pa-
moja na miti ya Edeni mpaka
nchi iliyo chini.[h] Utalala chi-
ni pamoja na wale walioiuawa
kwa upanga katikati ya
watu ambao hawajatahiriwa.
Huyu ni Farao na umati wake
wote,' asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova."

32 Na ikazidi kutukia kwa-
mba katika mwaka wa
kumi na mbili, katika mwe-
zi wa kumi na mbili, siku ya
kwanza ya mwezi huo, neno
la Yehova likanijia, na kuse-
ma: **2** "Mwana wa binadamu,
mfanyie wimbo wa huzuni Fa-
rao mfalme wa Misri, nawe
utamwambia, 'Umenyamazi-

Eze 31:16,* 17* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

SURA 31
a Isa 14:15
b Isa 14:8; Eze 31:9
c Eze 32:31
d Eze 32:21
e Omb 4:20; Eze 30:6; Eze 32:31
f Eze 32:19
g Eze 31:9
h 1Sa 2:7

Safu ya 2

SURA 32
a Met 28:15
b Isa 27:1; Isa 51:9; Eze 29:3
c Zb 66:11
d Mhu 9:12; Ho 7:12; Hab 1:17
e Eze 29:5
f Zb 63:10; Zb 79:2; Eze 29:5; Eze 39:17
g Eze 31:12
h Ufu 14:20
i Isa 13:10; Yoe 2:31; Amo 8:9; Mt 24:29; Ufu 6:12

shwa kama mwana-simba wa
mataifa mwenye manyoya shi-
ngoni.[a]
"'Nawe umekuwa kama mnya-
ma mkubwa wa majini katika
bahari,[b] nawe uliendelea kufo-
ka katika mito yako, nawe uka-
endelea kutibua maji kwa mi-
guu yako na kuichafua mito
yao.'
3 "Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova amesema hivi, 'Pia ni-
tatandaza juu yako wavu[c] wa-
ngu kwa kutumia kutaniko la
vikundi vingi vya watu, nao ha-
kika watakuleta katika wavu
wangu wa kukokota.[d] **4** Nami
nitakuacha juu ya nchi. Nita-
kutupa juu ya uso wa sha-
mba.[e] Nami nitavifanya viumbe
vyote vinavyoruka vya mbingu-
ni vikae juu yako, nami nita-
washibisha wanyama-mwitu wa
dunia nzima kutokana nawe.[f]
5 Nami nitaiweka nyama yako
juu ya milima na kuyajaza ma-
bonde kwa takataka zako.[g]
6 Nami nitaifanya nchi inywe
kilichokutoka, damu yako,[h] juu
ya milima; na vijito vitajazwa
kutokana nawe.'
7 "'Na wakati utakapozi-
mwa nitazifunika mbingu na
kuzitia giza nyota zake. Nalo
jua, nitalifunika kwa mawi-
ngu, na mwezi wenyewe ha-
utaacha nuru yake iangaze.[i]
8 Mianga yote ya nuru mbi-
nguni—nitaitia giza kwa saba-
bu yako, nami nitatia giza juu
ya nchi yako,' asema Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova.
9 "'Nami nitaitia uchungu
mioyo ya vikundi vingi vya
watu nitakapoleta mateka ku-
toka kwako katikati ya mataifa
mpaka nchi ambazo huku-

zijua.[a] **10** Nami nitafanya vikundi vingi vya watu waingiwe na hofu[b] kwa sababu yako, na wafalme wao watatetemeka kwa hofu kwa sababu yako wakati nitakapoutikisa upanga wangu usoni pao,[c] nao watatetemeka kila dakika, kila mmoja kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe, katika siku ya kuanguka kwako.'[d]

11 "Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Upanga wa mfalme wa Babiloni utakuja juu yako.[e] **12** Nitaufanya umati wako uanguke kwa panga za wenye nguvu, watu wa mataifa wenye kuonea, hao wote;[f] nao kwa kweli wataipora fahari ya Misri, na umati wake wote lazima uangamizwe.[g] **13** Nami nitaangamiza wanyama wake wote wa kufugwa kutoka kando ya maji mengi,[h] na mguu wa mtu wa udongo hautayatibua[i] tena, wala hata kwato za mnyama wa kufugwa hazitayatibua.'

14 "'Wakati huo nitayafanya maji yao yawe safi, na mito yao nitaifanya iende kama mafuta,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

15 "'Nitakapoifanya nchi ya Misri iwe mahame yenye ukiwa nayo nchi ifanywe ukiwa, isiwe na vitu vinavyoijaza,[j] nitakapowaua wakaaji wote waliomo ndani yake, pia watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.[k]

16 "'Huu ni wimbo wa huzuni, na hakika watu watauimba. Hata binti za mataifa watauimba; watauimba juu ya Misri na juu ya umati wake wote,'[l] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

17 Na ikazidi kutukia kwamba katika mwaka wa kumi na mbili, siku ya kumi na tano ya mwezi huo, neno la Yehova likanijia, na kusema: **18** "Mwana wa binadamu, ombolezea umati wa Misri na kuushusha chini,[a] yeye na binti za mataifa makuu, mpaka nchi iliyo chini,[b] pamoja na wale wanaoshuka kuingia shimoni.[c]

19 "'Wewe unapendeza zaidi kwa kulinganishwa na nani?[d] Shuka, nawe lazima ulazwe pamoja na watu ambao hawajatahiriwa!'[e]

20 "'Wataanguka katikati ya wale waliouawa kwa upanga.[f] Yeye ametiwa mkononi mwa upanga. Mkokoteeni mbali pamoja na umati wake wote.

21 "'Watu wa kwanza kabisa kati ya wenye nguvu watasema naye katikati ya Kaburi,* pamoja na wasaidizi wake.[g] Hakika watashuka chini;[h] watalala kama wale ambao hawajatahiriwa, waliouawa kwa upanga. **22** Huko ndiko aliko Ashuru pamoja na kutaniko lake lote.[i] Makaburi yake yanamzunguka pande zote. Hao wote wameuawa, wale wanaoanguka kwa upanga.[j] **23** Kwa maana makaburi yake yamewekwa katika sehemu za ndani kabisa za shimo,[k] na kutaniko lake linazunguka kaburi lake pande zote, hao wote wakiwa wameuawa, wakianguka kwa upanga, kwa sababu walikuwa wamesababisha hofu katika nchi ya walio hai.

Eze 32:21* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

SURA 32

a Eze 29:12
Eze 30:26

b Eze 27:35

c Kum 32:41

d Kut 15:14

e Yer 43:10
Yer 46:26
Eze 30:24

f Eze 30:11
Hab 1:6

g Eze 29:19

h Eze 29:8
Eze 30:12

i Eze 29:11

j Zb 107:34
Eze 29:12

k Kut 7:5
Kut 14:4
Zb 9:16
Eze 30:26

l 2Sa 1:17
2Nya 35:25

Safu ya 2

a Yer 1:10

b Zb 63:9
Eze 31:14

c Zb 30:9

d Eze 31:2

e Eze 28:10

f Eze 29:8

g Isa 14:9

h Zb 9:17
Zb 55:15

i Hes 24:24

j Isa 37:36
Zek 10:11

k Isa 14:15

24 "'Kuna Elamu[a] na umati wake wote kulizunguka kaburi lake pande zote, hao wote wakiwa wameuawa, wale wanaoanguka kwa upanga, ambao wameshuka chini wakiwa hawajatahiriwa mpaka nchi iliyo chini, wale ambao wamesababisha hofu yao katika nchi ya wale walio hai; nao watachukua fedheha yao pamoja na wale wanaoshuka kuingia katika shimo.[b] **25** Katikati ya waliouawa wameweka kitanda[c] kwa ajili yake katikati ya umati wake wote. Makaburi yake yanakizunguka pande zote. Hao wote hawajatahiriwa, wakiwa wameuawa kwa upanga,[d] kwa sababu hofu yao ilisababishwa katika nchi ya wale walio hai; nao watachukua fedheha yao pamoja na wale wanaoshuka kuingia katika shimo. Yeye amewekwa katikati ya waliouawa.

26 "'Mesheki[e] na Tubali[f] na umati wake wote wako huko. Makaburi yake yanamzunguka pande zote. Hao wote hawajatahiriwa, wakiwa wamechomwa kwa upanga, kwa sababu wamesababisha hofu yao katika nchi ya wale walio hai. **27** Nao je, hawatalala pamoja na wenye nguvu,[g] wanaoanguka kutoka kati ya watu ambao hawajatahiriwa, ambao wameshuka kuingia katika Kaburi* wakiwa na silaha zao za vita? Nao wataweka panga zao chini ya vichwa vyao, nayo makosa yao yatakuwa juu ya mifupa yao,[h] kwa sababu wenye nguvu walisababisha hofu katika nchi ya wale walio hai.[i]

28 Na wewe, utavunjwa katikati ya watu ambao hawajatahiriwa, nawe utalala chini pamoja na wale waliouawa kwa upanga.

29 "'Edomu,[a] wafalme wake na wakuu wake wote wako huko, ambao, katika nguvu zao, waliwekwa pamoja na wale waliouawa kwa upanga;[b] wao wenyewe watalala pamoja na watu ambao hawajatahiriwa[c] na pamoja na wale wanaoshuka kuingia katika shimo.

30 "'Watawala wadogo wa kaskazini wako huko, hao wote, na Wasidoni[d] wote, ambao wameshuka chini pamoja na wale waliouawa, katika utishaji wao kwa sababu ya nguvu zao, wakiwa wameona aibu. Nao watalala wakiwa hawajatahiriwa pamoja na wale waliouawa kwa upanga nao watachukua fedheha yao pamoja na wale wanaoshuka kuingia katika shimo.[e]

31 "'Hao ndio atakaowaona Farao, naye atafarijiwa juu ya umati wake wote.[f] Farao na jeshi lake lote watakuwa watu waliouawa kwa upanga,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

32 "'Kwa maana amesababisha hofu yake katika nchi ya walio hai,[g] naye atalazwa katikati ya watu ambao hawajatahiriwa, pamoja na wale waliouawa kwa upanga, yeye Farao na umati wake wote,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

33 **1** Nalo neno la Yehova likanijia, na kusema: **2** "Mwana wa binadamu, sema na wana wa watu wako,[h] nawe uwaambie,

SURA 32
a Mwa 10:22; Yer 49:34
b Eze 32:29
c Ayu 17:13
d 2Sa 1:19
e Mwa 10:2; Eze 27:13; Eze 38:2
f 1Nya 1:5; Eze 39:1
g Ayu 3:14; Isa 14:18
h Zb 92:9; Yoh 8:24
i Eze 32:23

Safu ya 2
a Mwa 25:30; Mwa 36:1; Isa 34:5; Eze 25:12; Amo 1:11; Oba 1; Mal 1:4
b Yer 25:31
c Yer 9:26
d Mwa 10:15; Eze 28:21
e Eze 32:24
f Eze 31:16
g Eze 32:27

SURA 33
h Eze 3:11

Eze 32:27* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

"'Kwa habari ya nchi, ikiwa nitauleta upanga[a] juu yake na watu wa nchi, kila mmoja, wamchukue mtu na kumweka kuwa mlinzi wao,[b] **3** naye kwa kweli aone upanga ukija juu ya nchi, naye apige baragumu na kuwaonya watu,[c] **4** na msikiaji kwa kweli asikie sauti ya baragumu lakini asitii onyo hata kidogo,[d] nao upanga uje na kumchukua, damu yake mwenyewe itakuwa juu ya kichwa chake.[e] **5** Aliisikia sauti ya baragumu, lakini hakutii onyo. Damu yake mwenyewe itakuwa juu yake binafsi. Na kama angetii onyo, nafsi yake ingeponyoka.[f]

6 "'Basi kwa habari ya mlinzi, kama akiuona upanga ukija naye kwa kweli asipige baragumu[g] na watu wasipate onyo lolote nao upanga uje na kuichukua nafsi kutoka kwao, hiyo itachukuliwa kwa sababu ya kosa lake yenyewe,[h] lakini damu yake nitaidai kutoka mkononi mwa mlinzi.'[i]

7 "Basi kwa habari yako wewe, Ee mwana wa binadamu, nimekufanya kuwa mlinzi kwa nyumba ya Israeli,[j] na kutoka katika kinywa changu lazima usikie neno na kuwapa onyo kutoka kwangu.[k] **8** Mimi ninapomwambia mtu mwovu, 'Wewe mwovu, hakika utakufa!'[l] lakini kwa kweli wewe usiseme ili kumwonya mwovu aiache njia yake,[m] yeye mwenyewe kwa kuwa ni mwovu atakufa katika kosa lake,[n] lakini damu yake nitaidai katika mkono wako. **9** Lakini kwa habari yako wewe, ikiwa kwa kweli utamwonya mwovu aiache njia yake ili ageuke na kuiacha lakini kwa kweli asigeuke na kuiacha njia yake, yeye mwenyewe atakufa katika kosa lake,[a] lakini wewe hakika utaiokoa nafsi yako.[b]

10 "Basi kwa habari yako wewe, Ee mwana wa binadamu, iambie nyumba ya Israeli, 'Ninyi mmesema hivi: "Kwa sababu maasi yetu na dhambi zetu ziko juu yetu nasi tunaozea humo,[c] basi tutawezaje kuendelea kuishi?"'[d] **11** Waambie, '"Kama ninavyoishi," asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, "Ninapendezwa, si na kifo cha mwovu,[e] bali kwamba mtu mwovu ageuke na kuiacha[f] njia yake na kwa kweli aendelee kuishi.[g] Geukeni, geukeni mziache njia zenu mbaya,[h] maana kwa nini mfe, Ee nyumba ya Israeli?"'[i]

12 "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, waambie wana wa watu wako, 'Uadilifu wenyewe wa mwadilifu hautamkomboa katika siku ya maasi yake.[j] Lakini kwa habari ya uovu wa mwovu, hautamtikisa katika siku atakapogeuka na kuuacha uovu wake.[k] Wala hata mtu yeyote mwenye uadilifu hataweza kuendelea kuishi kwa sababu ya huo siku ile atakapotenda dhambi.[l] **13** Ninapomwambia mwadilifu: "Hakika utaendelea kuishi," na yeye mwenyewe kwa kweli autegemee uadilifu wake mwenyewe na kutenda ukosefu wa haki,[m] matendo yake yote ya uadilifu hayatakumbukwa, lakini kwa ukosefu wake wa haki ambao ameutenda—atakufa kwa sababu ya huo.[n]

14 "'Ninapomwambia mwovu: "Hakika utakufa,"[o] naye

SURA 33

a Law 26:25
Yer 25:31
Eze 6:3
Eze 14:17
Eze 21:9
b 2Sa 18:24
2Fa 9:17
Isa 21:8
Yer 51:12
Ho 9:8
c Ne 4:18
Isa 58:1
Yer 4:5
Ho 8:1
d 2Nya 25:16
Met 29:1
Yer 6:17
Zek 1:4
e Law 20:9
1Fa 2:37
Eze 3:19
Mdo 18:6
Mdo 20:26
f 2Fa 6:10
Ebr 11:7
g Isa 56:10
h Eze 18:24
i Mwa 42:22
Eze 3:18
j Isa 62:6
Eze 3:17
k 2Nya 19:10
Yer 1:17
l Isa 3:11
Eze 18:4
m Met 24:12
Eze 13:9
n Hes 27:3
Met 11:21
Mhu 8:13

Safu ya 2

a Met 15:10
b Eze 3:19
Mdo 18:6
c Law 26:39
Isa 64:6
Eze 24:23
d Eze 37:11
e 2Sa 14:14
Eze 18:23
Lu 15:10
1Ti 2:4
f Isa 31:6
g Zb 130:7
h Met 1:23
Isa 55:7
Yer 3:22
Yer 25:5
Eze 14:6
Ho 14:1
Mdo 3:19
i Eze 18:31
2Pe 3:9
j Eze 3:20
Eze 18:24
k 1Fa 8:48
2Nya 7:14
Eze 18:21
l Eze 18:26
m Eze 3:20
Eze 18:24
2Pe 2:20
n Yer 18:10
Eze 18:4
o Isa 3:11
Eze 3:18
Lu 13:3

kwa kweli ageuke na kuiacha dhambi yake[a] na kuendelea kutenda haki na uadilifu,[b]
15 naye mwovu arudishe kitu kile kilichowekwa rehani,[c] alipe vitu vile vilivyochukuliwa kwa unyang'anyi,[d] naye kwa kweli atembee katika sheria za uzima kwa kutotenda ukosefu wa haki,[e] hakika ataendelea kuishi.[f] Yeye hatakufa. **16** Hakuna yoyote kati ya dhambi zake alizozitenda itakayokumbukwa juu yake.[g] Yeye ameendelea kutenda haki na uadilifu. Hakika ataendelea kuishi.'[h]

17 "Nao wana wa watu wako wamesema, 'Njia ya Yehova si sawa,'[i] lakini, wao, njia yao ndiyo ambayo si sawa.

18 "Mtu mwadilifu anapogeuka na kuuacha uadilifu wake na kwa kweli atende kwa njia isiyo ya haki, lazima pia afe kwa sababu hiyo.[j] **19** Na mwovu anapogeuka na kuuacha uovu wake na kuendelea kutenda haki na uadilifu, yeye ataendelea kuishi kwa sababu ya hayo.[k]

20 "Nanyi mmesema, 'Njia ya Yehova si sawa.'[l] Nitawahukumu ninyi kila mmoja wenu kulingana na njia zake,[m] Ee nyumba ya Israeli."

21 Mwishowe ikatukia kwamba katika mwaka wa kumi na mbili, katika mwezi wa kumi, siku ya tano ya mwezi wa uhamisho wetu, mtu aliyeponyoka kutoka Yerusalemu akanijia,[n] akisema: "Jiji limepigwa na kuangushwa!"[o]

22 Basi mkono wa Yehova ulikuwa juu yangu wakati wa jioni kabla ya kuja kwa huyo aliyeponyoka,[p] na Yeye akakifungua kinywa changu kabla ya huyo kunijia wakati wa asubuhi, nacho kinywa changu kilikuwa kimefunguliwa nami sikuwa bubu tena.[a]

23 Nalo neno la Yehova likaanza kunijia, likisema:
24 "Mwana wa binadamu, wakaaji wa mahali hapa palipoharibiwa[b] wanasema hata juu ya udongo wa Israeli, 'Abrahamu alikuwa mmoja tu, hata hivyo aliitwaa nchi hii.[c] Na sisi ni wengi; tumepewa nchi hii iwe mali yetu.'[d]

25 "Kwa hiyo waambie, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Mnaendelea kula pamoja na damu,[e] nayo macho yenu mnaendelea kuyainua kuelekea sanamu zenu za mavi,[f] nanyi mnaendelea kuimwaga damu.[g] Kwa hiyo je, mnapaswa kuimiliki nchi hii?[h] **26** Mmeutegemea upanga wenu.[i] Mmefanya chukizo,[j] na kila mmoja wenu amemtia unajisi mke wa mwenzake.[k] Kwa hiyo je, mnapaswa kuimiliki nchi hii?"'[l]

27 "Unapaswa kuwaambia hivi, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Kama ninavyoishi, hakika wale walio katika mahali palipoharibiwa wataanguka kwa upanga;[m] na yule aliye katika shamba, hakika nitamfanya awe chakula cha mnyama-mwitu;[n] na wale walio katika mahali imara na katika mapango[o] watakufa kwa tauni.
28 Nami kwa kweli nitaifanya nchi iwe mahame yenye ukiwa,[p] naam, ukiwa, na fahari ya nguvu zake itakomeshwa[q] na milima ya Israeli itafanywa

SURA 33

a Met 28:13
Isa 55:7
Mdo 3:19
b Eze 18:21
Mik 6:8
c Kut 22:26
Eze 18:7
d Law 6:2
Eze 22:29
e Law 18:5
Law 19:15
f Eze 18:27
g Isa 1:18
h Eze 20:11
i Ayu 34:10
Ayu 40:8
Zb 92:15
Ro 3:4
j Ebr 10:38
2Pe 2:20
k Eze 18:27
l Met 19:3
Isa 55:8
Isa 55:9
Eze 18:25
Eze 18:29
m Mwa 18:25
Zb 62:12
Met 24:12
Ro 2:6
n Eze 24:26
o 2Fa 25:4
2Nya 36:17
Yer 39:2
p Eze 3:22

Safu ya 2

a Eze 3:26
b Yer 39:10
Eze 36:4
c Mwa 12:7
Isa 51:2
Mdo 7:5
d Mik 3:11
Mt 3:9
Yoh 8:39
e Mwa 9:4
Law 17:12
Kum 12:16
1Sa 14:32
Mdo 15:29
f Eze 18:6
g Eze 22:6
h Yer 7:10
Yer 44:22
i Mik 2:1
j Yer 17:5
Sef 3:3
k Yer 5:8
Ebr 13:4
l Kum 4:26
Yos 23:15
m Yer 15:2
Yer 42:22
Eze 5:12
n Eze 39:4
Ufu 19:18
o Amu 6:2
1Sa 13:6
p 2Nya 36:21
Isa 6:11
Yer 9:11
Yer 44:2
Eze 36:34
Mik 7:13
q Eze 24:21

ukiwa,[a] pasipo mtu anayepita katikati. **29** Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapoifanya nchi iwe mahame yenye ukiwa,[b] naam, ukiwa, kwa sababu ya machukizo yote ambayo wamefanya.”’[c]

30 “Na wewe, Ee mwana wa binadamu, wana wa watu wako wanasemezana juu yako kando ya kuta na katika miingilio ya nyumba,[d] na mmoja amesema na mwingine, kila mmoja na ndugu yake, na kusema, ‘Njooni, tafadhali, msikie ni neno gani linalotoka kwa Yehova.’[e] **31** Nao wataingia ndani kwako, kama wanavyoingia watu, na kuketi mbele yako kama watu wangu;[f] nao hakika watayasikia maneno yako lakini hawatayatenda,[g] kwa maana wanaonyesha tamaa zenye uchu kwa kinywa chao nao moyo wao unafuatilia pato lao lisilo la haki.[h] **32** Na, tazama! kwao wewe ni kama wimbo wa mapendo yenye hisia, kama mtu mwenye sauti nzuri na mwenye kupiga kinanda vizuri.[i] Nao hakika watayasikia maneno yako, lakini hakuna yeyote anayeyatenda.[j] **33** Na yatakapotimia—tazama! lazima yatatimia[k]—wao pia watalazimika kujua kwamba nabii alikuwa katikati yao.”[l]

34 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** “Mwana wa binadamu, toa unabii juu ya wachungaji wa Israeli. Toa unabii, nawe uwaambie hao wachungaji, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: “Ole wao wachungaji wa Israeli,[a] ambao wamekuwa watu wanaojilisha wenyewe![b] Je, wachungaji hawapaswi kulisha kundi?[c] **3** Mnakula mafuta,[d] na kujivika sufu ninyi wenyewe. Mnamchinja mnyama aliyenona.[e] Hamlishi kundi lenyewe. **4** Walio wagonjwa hamkuwatia nguvu,[f] na anayeugua hamkumponya, na aliyevunjika hamkumfunga, na aliyefukuzwa hamkumrudisha, na aliyepotea hamkumtafuta apatikane,[g] lakini mmewatawala kwa ukali, naam, kwa uonevu.[h] **5** Nao wakatawanyika hatua kwa hatua kwa sababu hapakuwa na mchungaji,[i] hivi kwamba wakawa chakula cha kila mnyama wa mwituni, nao wakaendelea kutawanyika.[j] **6** Kondoo zangu waliendelea kupotea kwenye milima yote na juu ya kila kilima kirefu;[k] na juu ya uso wote wa dunia kondoo zangu[l] walitawanyika, pasipo mtu wa kutafuta wala mtu anayejitahidi kupata.

7 “‘“Kwa hiyo, ninyi wachungaji, lisikieni neno la Yehova, **8** ‘“Kama ninavyoishi,” asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, “hakika kwa sababu kondoo zangu walikuwa kitu cha kuporwa na kondoo zangu waliendelea kuwa chakula kwa ajili ya kila mnyama wa mwituni, kwa sababu hapakuwa na mchungaji yeyote, nao wachungaji wangu hawakuwatafuta kondoo zangu, bali wachungaji waliendelea kujilisha wenyewe,[m] nao hawakuwalisha kondoo zangu,”’ **9** kwa hiyo, ninyi wachungaji, lisikieni neno la Yehova.

SURA 33

a Eze 6:3
b Zb 9:16
Yer 9:11
Yer 25:11
Yer 32:43
c 2Fa 17:9
2Nya 36:14
d Yer 11:19
Yer 18:18
e Mt 15:8
f Eze 8:1
Eze 20:1
g Isa 29:13
Yer 6:16
Yer 44:17
Mt 7:21
Lu 6:49
h Mt 6:24
i Mk 6:20
j Yak 1:22
k Yos 23:14
Isa 55:11
l 2Fa 5:8
Eze 2:5

Safu ya 2

SURA 34

a Yer 23:1
Mik 3:1
Mik 3:11
Sef 3:3
Zek 11:17
Mt 23:13
b Yud 12
c Isa 40:11
Yoh 21:15
d Isa 56:11
e 2Fa 21:16
Yer 22:17
Eze 34:20
Mik 3:3
Zek 11:5
f Zek 11:16
Mt 9:36
g Mt 10:6
Lu 15:4
h Yer 22:13
i 1Fa 22:17
Yer 23:2
Yer 50:6
Mt 9:36
Mk 6:34
j Isa 56:9
Yer 23:1
k Eze 7:16
l Zb 23:1
m Yud 12

10 Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova amesema hivi, 'Tazama
niko dhidi ya wachungaji,[a]
na hakika mimi nitadai kondoo
zangu kutoka mkononi mwao
na kuwafanya waache kuwali-
sha kondoo zangu,[b] nao wachu-
ngaji hawatajilisha tena ka-
mwe;[c] nami nitawakomboa ko-
ndoo zangu kutoka kinywani
mwao, nao hawatakuwa cha-
kula chao.'"[d]
11 "'Kwa maana Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova
amesema hivi: "Mimi nipo
hapa, mimi mwenyewe, nami
nitawatafuta kondoo zangu na
kuwatunza.[e] **12** Kulingana
na utunzaji wa mtu anayeli-
sha kundi[f] lake katika siku
ya kuja kwake kuwa katika-
ti ya kondoo zake ambao wa-
metawanyika kotekote,[g] hi-
vyo ndivyo nitakavyowatu-
nza kondoo zangu; nami ni-
tawakomboa kutoka mahali
pote ambapo wametawanyi-
ka katika siku ya mawingu na
giza zito.[h] **13** Nami nitawa-
toa[i] kutoka kwa vikundi vya
watu na kuwakusanya pamo-
ja kutoka katika zile nchi na
kuwaleta kwenye nchi yao[j]
na kuwalisha kwenye milima
ya Israeli, kando ya vijito na
kando ya makao yote ya nchi.[k]
14 Katika malisho mazuri ni-
tawalisha wao, na makao yao
yatakuwa katika milima mi-
refu ya Israeli.[l] Huko wata-
lala katika makao mazuri,[m]
na kwenye malisho manono
watajilisha juu ya milima ya
Israeli."
15 "'"Mimi mwenyewe ni-
tawalisha kondoo zangu,[n] na
mimi mwenyewe nitawalaza,"[o]
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova. **16** "Aliyepotea
nitamtafuta, na aliyefukuzwa
nitamrudisha,[a] na aliyevunji-
ka nitamfunga na anayeugua
nitamtia nguvu, lakini aliye-
nona[b] na aliye na nguvu ni-
tamwangamiza. Huyo nitamli-
sha hukumu."[c]
17 "'Nanyi kondoo zangu,
Bwana Mwenye Enzi Kuu Yeho-
va amesema hivi: "Tazama, ni-
nahukumu kati ya kondoo na
kondoo, kati ya kondoo-dume
na mbuzi-dume.[d] **18** Je, ni ja-
mbo dogo kwenu kwamba ninyi
mnajilisha malisho yaliyo bora
zaidi[e] lakini yale malisho mengi-
ne yenu mnayakanyaga-kanya-
ga kwa miguu yenu, na kwamba
maji safi mnayanywa lakini ya-
liyobaki mnayachafua kwa ku-
yakanyaga-kanyaga kwa miguu
yenu? **19** Nao kondoo zangu,
je, wajilishe kwenye malisho
mliyokanyaga-kanyaga kwa mi-
guu yenu na kunywa maji yali-
yochafuliwa kwa kukanyagwa-
kanyagwa kwa miguu yenu?"
20 "'Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amewaam-
bia hivi: "Tazama mimi nipo
hapa, mimi mwenyewe, nami ni-
tahukumu kati ya kondoo ali-
yenona na kondoo aliyeko-
nda, **21** kwa sababu kwa
ubavu na kwa bega mliende-
lea kusukuma na kwa pembe
zenu mliendelea kuwasukuma
wote waliofanywa kuwa wago-
njwa mpaka mkawa mmewata-
wanya nje.[f] **22** Nami nitawa-
okoa kondoo zangu, nao ha-
wataendelea kuwa tena kitu
cha kuporwa;[g] nami nitahuku-
mu kati ya kondoo na kondoo.
23 Nami nitasimamisha juu yao
mchungaji mmoja,[h] naye atawa-

SURA 34
a Eze 13:8
Zek 10:3
b Yer 52:24
Yer 52:27
c 1Sa 2:29
d Zb 72:12
e Zb 80:1
Isa 56:8
f 1Sa 17:35
g Isa 40:11
h Eze 30:3
Yoe 2:2
Sef 1:15
i 1Pe 2:25
j Zb 106:47
Isa 65:9
Yer 23:3
Yer 30:3
Eze 11:17
Eze 28:25
Amo 9:14
k Mik 7:14
l Zb 23:2
Isa 25:6
Isa 30:23
Yer 31:12
m Yer 33:12
n Zb 23:1
Yer 3:15
o Sef 3:13

Safu yen a 2
a Mik 4:6
Mt 15:24
Lu 15:4
b Kum 32:15
Isa 10:16
Amo 4:1
c Isa 49:26
Yer 9:15
d Isa 34:6
Yer 51:40
Zek 10:3
Mt 25:33
e Mik 2:2
f Zek 11:5
Zek 11:16
Lu 13:14
g Zb 72:12
Isa 40:11
Yer 23:3
Zek 11:7
h Mhu 12:11
Yer 23:4
Yoh 10:11
Ebr 13:20
1Pe 5:4
Ufu 7:17

lisha, naam, mtumishi wangu Daudi.[a] Yeye mwenyewe atawalisha, na yeye mwenyewe atakuwa mchungaji wao.[b] **24** Na mimi mwenyewe, Yehova, nitakuwa Mungu wao,[c] na mtumishi wangu Daudi atakuwa mkuu katikati yao.[d] Mimi mwenyewe, Yehova, nimesema.

25 "'"Nami nitafanya agano la amani pamoja nao,[e] na hakika mimi nitamkomesha katika nchi mnyama-mwitu mwenye kudhuru,[f] nao kwa kweli watakaa nyikani kwa usalama na kulala katika misitu.[g] **26** Nami nitawafanya wao na mazingira ya kilima changu kuwa baraka,[h] nami nitaifanya mvua inayomwagika ishuke kwa wakati wake. Kutakuwa na mvua inayomwagika ya baraka.[i] **27** Na mti wa shambani utatoa matunda[j] yake, na nchi yenyewe itatoa mazao[k] yake, nao kwa kweli watakuwa katika nchi yao kwa usalama.[l] Nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapovunja nira[m] zao na kuwakomboa kutoka katika mkono wa wale waliokuwa wakiwatumia kama watumwa.[n] **28** Nao hawataendelea kuwa kitu cha kuporwa na mataifa;[o] na kwa habari ya mnyama-mwitu wa dunia, yeye hatawararua, nao kwa kweli watakaa katika usalama, pasipo mtu yeyote wa kuwatetemesha.[p]

29 "'"Nami nitawainulia mmea ili kujifanyia jina,[q] nao hawatakuwa tena wale waliondolewa na njaa katika nchi,[r] nao hawatachukua fedheha tena kamwe kutoka kwa mataifa.[s] **30** 'Nao watalazimika kujua kwamba mimi, Yehova Mungu wao, niko pamoja nao[a] na kwamba wao ni watu wangu, nyumba ya Israeli,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."'[b]

31 "'Na kwa habari yenu ninyi kondoo zangu,[c] kondoo wa malisho yangu, ninyi ni watu wa udongo. Mimi ni Mungu wenu,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

35 Na neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** "Mwana wa binadamu, elekeza uso[d] wako kwenye eneo lenye milima la Seiri[e] na utoe unabii juu yake.[f] **3** Nawe utaliambia, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Mimi hapa niko dhidi yako, Ee eneo lenye milima la Seiri,[g] nami nitaunyoosha mkono wangu juu yako[h] na kukufanya uwe mahame, naam, kuwa ukiwa.[i] **4** Majiji yako nitayafanya kuwa mahali palipoharibiwa, na wewe mwenyewe utakuwa mahame yenye ukiwa;[j] nawe utalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova,[k] **5** kwa sababu ulikuwa na uadui wenye kudumu mpaka wakati usio na kipimo[l] nawe uliendelea kuwatia wana wa Israeli kwenye nguvu za upanga,[m] wakati wa maafa yao,[n] wakati wa kosa lao la mwisho."'[o]

6 "'Kwa hiyo kama ninavyoishi,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'kwa sababu nilikuwa nikikutayarisha kwa ajili ya damu, damu yenyewe pia itakufuatilia wewe.[p]

SURA 34
a Isa 11:1; Isa 55:3; Yer 30:9
b Eze 37:24; Ho 3:5
c Mwa 17:7; Kut 29:45; Yer 31:1; Zek 13:9
d Zb 2:6; Isa 9:6; Yer 23:5; Mik 5:2; Lu 1:32; Mdo 5:31
e Isa 55:3; Eze 37:26
f Law 26:6; Isa 11:6; Isa 35:9; Isa 65:25; Ho 2:18
g Zb 4:8; Yer 23:6; Yer 33:16
h Isa 56:7; Eze 20:40; Mik 4:1
i Mwa 12:2; Law 26:4; Kum 28:12; Zb 68:9; Met 10:22; Zek 8:13; Mal 3:10
j Law 26:4; Isa 35:2; Isa 55:12
k Zb 85:12; Eze 36:30
l Law 25:18
m Law 26:13; Yer 2:20; Eze 30:18
n Yer 25:14
o Yer 30:10; Eze 36:4
p Yer 46:27
q Zb 72:7; Isa 11:1
r Eze 36:29
s Eze 36:15

Safu ya 2
a Zb 46:7; Eze 37:27
b Ro 9:25
c Zb 78:52; Zb 100:3; Isa 40:11; 1Pe 5:2

SURA 35
d Eze 6:2
e Mwa 32:3; Kum 2:5; Eze 25:8
f Yer 49:8; Omb 4:22; Eze 36:5; Amo 1:11; Oba 1; Oba 10
g Eze 25:12
h Yer 6:12
i Eze 25:13
j Yoe 3:19; Mal 1:3
k Zb 9:16
l Mwa 27:41
m Amo 1:11
n Oba 10
o Zb 137:7
p Zb 109:16; Oba 15; Ro 2:6; Ga 6:7.

Hakika damu ndiyo uliyoichukia, na damu yenyewe ndiyo itakayokufuatilia.[a] **7** Nami hakika nitalifanya eneo lenye milima la Seiri kuwa mahame, naam, kuwa ukiwa,[b] nami nitamkatilia mbali kutoka hilo mtu yeyote anayepita katikati na mtu anayerudi.[c] **8** Nami nitaijaza milima yake kwa watu wake walioiuawa; na katika vilima vyako na mabonde yako na vijito vyako vyote, wale walioiuawa kwa upanga watananguka humo.[d] **9** Nitakufanya kuwa mahame yenye ukiwa yanayodumu mpaka wakati usio na kipimo, nayo majiji yako mwenyewe hayatakaliwa;[e] nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova."[f]

10 "Kwa sababu ulisema, 'Mataifa haya mawili na nchi hizi mbili—zitakuwa zangu mwenyewe, nasi hakika tutaitwaa kila nchi,'[g] ijapokuwa Yehova mwenyewe alikuwa hapo,[h] **11** 'kwa hiyo kama ninavyoishi,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'nitatenda pia kulingana na hasira yako na kulingana na wivu wako ambao umeonyesha kwa sababu ya hisia zako za chuki kuwaelekea;[i] nami nitajijulisha mwenyewe katikati yao nitakapokuhukumu.[j] **12** Nawe utalazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova, nimesikia mambo yako yote yasiyo ya heshima ambayo umesema kuhusu milima ya Israeli,[k] ukisema: "Imefanywa ukiwa. Imetiwa mkononi mwetu iwe chakula chetu."[l] **13** Nanyi mliendelea kutenda kwa majivuno makubwa juu yangu kwa vinywa vyenu,[m] nanyi mmezidisha maneno yenu juu yangu.[a] Mimi mwenyewe nimeyasikia.'[b]

14 "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Wakati uleule ambao dunia yote inashangilia, nitakufanya wewe kuwa mahame yenye ukiwa. **15** Kama vile tu ulivyoshangilia urithi wa nyumba ya Israeli kwa sababu ilifanywa ukiwa, nitakutendea jambo hilohilo.[c] Utakuwa mahame yenye ukiwa, Ee eneo lenye milima la Seiri, naam, Edomu yote, naam, yote pia;[d] nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.'"[e]

36 "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, toa unabii juu ya milima ya Israeli, nawe utasema, 'Ee milima ya Israeli,[f] lisikieni neno la Yehova. **2** Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Kwa sababu adui amesema juu yenu,[g] 'Aha! Hata mahali pa juu pa wakati wa kale[h]—pamekuwa mali yetu!'"'[i]

3 "Kwa hiyo toa unabii, nawe utasema, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Kwa sababu, naam, kwa sababu kumekuwa na kufanywa ukiwa[j] na kuumwa kutoka pande zote,[k] ili muwe mali ya mabaki ya mataifa[l] nanyi mnaendelea kusemwa kwa midomo[m] na kati ya watu kuna habari mbaya,[n] **4** kwa hiyo, enyi milima ya Israeli,[o] lisikieni neno la Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova! Ni hivi Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova ameambia milima na vilima, vijito na mabonde na mahali palipoharibiwa[p] na kufanywa ukiwa na

SURA 35
a Zb 109:17; Eze 25:14
b Eze 25:13
c Amu 5:6; Eze 29:11
d Isa 34:2; Yer 25:33
e Yer 49:17; Yer 49:18; Eze 25:13; Mal 1:4
f Zb 9:16
g Zb 83:4; Eze 36:5; Oba 13
h Zb 48:1; Eze 48:35; Sef 3:15
i Law 19:17; Zb 37:7; Amo 1:11; Mt 7:2; 1Yo 3:15
j Met 11:21; Isa 26:9
k Zb 94:9
l Zb 83:12; Eze 36:2
m 1Sa 2:3; 2Nya 32:15; Da 11:36; Ufu 13:6

Safu ya 2
a Oba 3
b 2Fa 19:28; Yer 29:23
c Met 17:5; Omb 4:21; Oba 12; Oba 15
d Isa 34:5; Eze 25:13; Eze 36:5
e Zb 9:16

SURA 36
f Eze 6:2
g Eze 25:3
h Kum 32:13; Zb 78:69; Isa 58:14
i Yer 49:1; Eze 35:10
j Law 26:43
k Amo 8:4
l Eze 25:4
m Kum 28:37; Zb 44:13; Yer 18:16; Omb 2:15; Da 9:16
n 1Fa 9:7
o Isa 44:23; Isa 49:13; Eze 6:2
p Yer 25:9

majiji yaliyoachwa ambayo ya-
meporwa na kudhihakiwa na
mabaki ya mataifa yanayo-
zunguka pande zote;[a] **5** kwa
hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu
Yehova amesema hivi, 'Hakika katika moto wa bidii yangu nitasema[b] juu ya mabaki ya mataifa na juu ya Edomu yote,[c] wale ambao wamejipatia wenyewe nchi yangu iwe mali yao kwa kushangilia kwa moyo wote,[d] kwa dharau katika nafsi yao,[e] kwa ajili ya kiwanja chake cha malisho na ili kuipora.'"'[f]

6 "Kwa hiyo toa unabii kuhusu udongo wa Israeli, nawe utaambia milima na vilima, vijito na mabonde, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Tazama! mimi mwenyewe katika bidii yangu na katika ghadhabu yangu lazima nitasema, kwa sababu mmechukua fedheha ya mataifa."'[g]

7 "Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Mimi mwenyewe nimeuinua mkono wangu katika kiapo[h] ili mataifa yanayowazunguka pande zote—hayo yatachukua fedheha yao yenyewe.[i] **8** Na ninyi wenyewe, enyi milima ya Israeli, mtatoa matawi yenu wenyewe na kuzaa matunda yenu wenyewe kwa ajili ya watu wangu Israeli,[j] kwa maana wamekaribia hatua ya kuingia ndani.[k] **9** Kwa maana tazama, nimewapa ninyi kibali changu, nami hakika nitageuka kuwaelekea ninyi,[l] na kwa kweli ninyi mtalimwa na kupandwa mbegu.[m] **10** Nami nitazidisha binadamu juu yenu, nyumba yote ya Israeli, naam, nyumba yote,[n] na majiji yatakaliwa,[a] na mahali palipoharibiwa penyewe patajengwa upya.[b] **11** Naam, nitawazidisha binadamu na wanyama juu yenu,[c] nao hakika wataongezeka na kuzaa, nami kwa kweli nitawafanya ninyi mkaliwe kama ilivyokuwa hali yenu ya zamani[d] nami nitafanya mema zaidi kuliko ilivyokuwa hali yenu ya zamani;[e] nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.[f] **12** Na juu yenu nitawafanya binadamu watembee, naam, watu wangu Israeli, nao watawamiliki ninyi,[g] nanyi mtakuwa fungu lao la urithi,[h] nanyi hamtawaua[i] watoto wao tena.'"

13 "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Kwa sababu kuna wale wanaowaambia ninyi: "Wewe ni mmezaji wa binadamu, nawe umekuwa nchi inayowaua watoto wa mataifa yako,"'[j] **14** 'kwa hiyo hutawameza binadamu tena,[k] nawe hutawaua watoto wa mataifa yako tena,'[l] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. **15** 'Nami sitasababisha tena mazungumzo zaidi yenye kufedhehesha ya mataifa yasikiwe juu yako,[m] nawe hutachukua tena shutuma ya watu,[n] nayo mataifa yako hutayafanya yajikwae tena,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

16 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **17** "Mwana wa binadamu, nyumba ya Israeli walikuwa wakikaa katika nchi yao, nao wakaendelea kuichafua kwa njia yao na kwa matendo yao.[o] Njia yao imekuwa mbele zangu kama uchafu wa

SURA 36

a Zb 79:4
Eze 34:28
b Kum 4:24
Isa 66:15
Eze 38:19
Sef 3:8
c Zek 1:15
d Zb 83:4
Eze 35:10
e Met 17:5
Oba 12
f Eze 25:12
Amo 1:11
g Zb 74:10
Zb 123:4
Eze 34:29
h Kum 32:40
Eze 20:5
Eze 20:15
i Yer 25:9
Yer 49:17
Amo 1:11
j Zb 98:8
Isa 44:23
Isa 51:3
Isa 60:5
Eze 36:30
k Isa 2:3
l Sef 3:9
m Hag 2:19
n Yer 30:19

Safu ya 2

a Zek 8:4
b Isa 51:3
Isa 58:12
Isa 61:4
Amo 9:14
c Yer 31:27
Yer 33:12
d Yer 30:18
e Isa 54:7
Eze 37:6
Hag 2:9
f Ho 2:20
Yoe 3:17
g Yer 32:44
Oba 17
h Isa 60:21
i Isa 65:23
Yer 15:7
j Yer 15:7
k Met 30:14
l Yer 32:35
m Isa 54:4
Isa 60:14
Eze 34:29
Mik 7:8
Sef 3:19
n Zb 89:50
Eze 36:20
Eze 36:21
Sef 2:8
o Law 18:25
Zb 106:38
Isa 24:5
Yer 2:7
Yer 3:1
Yer 16:18

hedhi.[a] **18** Nami nikamwa-
ga ghadhabu yangu juu yao
kwa sababu ya damu waliyoku-
wa wameimwaga juu ya nchi,[b]
nchi ambayo walikuwa wamei-
chafua kwa sanamu zao za
mavi.[c] **19** Nami nikawatawa-
nya katikati ya mataifa, hivi
kwamba wakasambaa katika
nchi mbalimbali.[d] Niliwahuku-
mu kulingana na njia yao na
kulingana na matendo yao.[e]
20 Kwa hiyo wakaingia kwa
mataifa ambamo waliingia, na
watu wakatia unajisi jina la-
ngu takatifu[f] kwa kusema hivi
juu yao, 'Hawa ndio watu wa
Yehova, nao wametoka kati-
ka nchi yake.'[g] **21** Nami nita-
lihurumia jina langu takatifu,
ambalo nyumba ya Israeli ime-
litia unajisi katikati ya mataifa
ambamo wameingia."[h]

22 "Kwa hiyo iambie nyu-
mba ya Israeli, 'Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amese-
ma hivi: "Sifanyi jambo hili
kwa ajili yenu, Ee nyumba ya
Israeli, bali kwa ajili ya jina
langu takatifu, ambalo ninyi
mmelitia unajisi katikati ya
mataifa ambamo mmeingia."'[i]
23 'Nami hakika nitalitaka-
sa jina langu kuu,[j] ambalo li-
likuwa likitiwa unajisi kati-
kati ya mataifa, ambalo ni-
nyi mlilitia unajisi katikati yao;
nayo mataifa yatalazimika ku-
jua kwamba mimi ni Yehova,'[k]
asema Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova, 'wakati nitaka-
potakaswa katikati yenu mbe-
le ya macho yao.[l] **24** Nami ni-
tawatoa ninyi kutoka kwa ma-
taifa na kuwakusanya pamo-
ja kutoka katika nchi zote na
kuwaingiza katika nchi yenu.[m]
25 Nami nitawanyunyizia maji

SURA 36

a Law 12:2
Isa 64:6
b 2Nya 34:21
Isa 42:25
c Eze 23:37
d Law 26:38
Kum 28:64
Eze 22:15
e Eze 7:3
Eze 18:30
Eze 39:24
f Isa 52:5
Ro 2:24
g Hes 14:16
Yos 7:9
h Kut 20:7
Zb 74:18
Isa 48:9
Isa 52:5
Eze 20:9
i Zb 106:8
j Zb 46:10
Isa 5:16
Eze 20:41
k Zb 102:15
l Eze 28:22
m Kum 30:3
Isa 43:5
Yer 23:3
Eze 34:13
Eze 37:21
Ho 1:11

Safu ya 2

a Hes 19:13
Zb 51:7
Ebr 10:22
b Isa 4:4
Yer 33:8
1Ko 6:11
c Eze 6:4
d Kum 30:6
Yer 32:39
Eze 11:19
e Zb 51:10
f Zek 7:12
g Isa 44:3
Yoe 2:28
h Yer 31:33
i Eze 11:20
j Eze 28:25
Eze 37:25
k Yer 30:22
Eze 11:20
Eze 37:27
l Mt 1:21
Ro 11:26
m Zb 33:19
Eze 34:29
n Eze 34:27
Eze 36:8
Eze 36:35
o Law 26:39
Ezr 9:6
Ne 9:26
Yer 31:18
p Eze 6:9
Eze 20:43
Zek 12:10
q Kum 9:5
Da 9:19
r Ro 6:21

safi, nanyi mtakuwa safi;[a] nami
nitawasafisha ninyi kutokana
na uchafu[b] wenu wote na ku-
tokana na sanamu zenu zote
za mavi.[c] **26** Nami nitawa-
pa ninyi moyo mpya,[d] na ni-
tatia ndani yenu roho mpya,[e]
nami nitauondoa moyo wa jiwe
kutoka mwilini mwenu na ku-
wapa ninyi moyo wa nyama.[f]
27 Nami nitaitia roho yangu
ndani yenu,[g] nami nitachu-
kua hatua ili mtembee kati-
ka masharti yangu,[h] nayo ma-
amuzi yangu ya hukumu mta-
yashika na kuyafanya kikwe-
li.[i] **28** Nanyi hakika mtakaa
katika nchi niliyowapa maba-
bu zenu,[j] nanyi mtakuwa watu
wangu na mimi mwenyewe ni-
takuwa Mungu wenu.'[k]

29 "'Nami nitawaokoa ni-
nyi kutoka kwenye uchafu[l]
wenu wote na kuiita nafaka
na kuifanya iwe tele, nami si-
taweka juu yenu njaa yoyote.[m]
30 Nami hakika nitafanya ma-
tunda ya mti yawe tele, na ma-
zao ya shamba, ili msishutu-
miwe tena na mataifa kwa sa-
babu ya njaa.[n] **31** Nanyi mta-
kumbuka njia zenu mbaya na
matendo yenu ambayo hayaku-
wa mazuri,[o] nanyi mtachuki-
zwa na nafsi zenu wenyewe
kwa sababu ya makosa yenu
na kwa sababu ya machukizo
yenu.[p] **32** Sifanyi jambo hili
kwa ajili yenu,'[q] asema Bwa-
na Mwenye Enzi Kuu Yehova,
'na ijulikane kwenu. Mwone
aibu na kufedheheka kwa sa-
babu ya njia zenu, Ee nyumba
ya Israeli.'[r]

33 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi,
'Siku nitakayowasafisha ninyi

kutokana na makosa yenu yote
nitayafanya pia majiji yakaliwe,[a] na mahali palipoharibiwa
patajengwa upya.[b] **34** Nayo
nchi iliyofanywa ukiwa italimwa, ingawa ilikuwa imekuwa mahame yenye ukiwa
machoni pa kila mpita-njia.[c]
35 Na hakika watasema: "Ile nchi kule ambayo ilifanywa ukiwa imekuwa kama
bustani ya Edeni,[d] nayo majiji yaliyokuwa ukiwa na ambayo yalikuwa yamebomolewa
yametiwa ngome; yamekaliwa."[e] **36** Nayo mataifa yatakayokuwa yamebaki kuwazunguka ninyi pande zote yatalazimika kujua kwamba mimi
mwenyewe, Yehova, nimejenga vitu vilivyobomolewa,[f] nimepanda kilichofanywa ukiwa. Mimi mwenyewe, Yehova,
nimesema nami nimelitenda.'[g]

37 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi,
'Hili ndilo bado nitajiacha niulizwe na nyumba ya Israeli
ili niwafanyie:[h] Mimi nitawazidisha kwa watu kama kundi.[i]
38 Kama kundi la watu watakatifu, kama kundi la Yerusalemu katika majira yake ya sherehe,[j] hivyo ndivyo majiji yaliyokuwa yamefanywa ukiwa
yatakavyojaa kundi la watu;[k]
nao watu watalazimika kujua
kwamba mimi ni Yehova.'"

37 Mkono wa Yehova ulikuwa juu yangu,[l] hivi kwamba akanichukua katika roho
ya Yehova[m] na kuniweka chini katikati ya nchi tambarare
ya bondeni, nayo ilikuwa imejaa mifupa.[n] **2** Naye akanipitisha kando yake pande zote,
na, tazama! ilikuwa mingi sana
kwenye uso wa hiyo nchi tambarare ya bondeni na, tazama!
ilikuwa mikavu sana.[a] **3** Naye
akaanza kuniambia: "Mwana wa binadamu, je, mifupa hii inaweza kuwa hai?" Nikajibu:
"Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, wewe mwenyewe unajua vema."[b] **4** Naye akaendelea kuniambia: "Toa unabii juu
ya mifupa hii, nawe uiambie,
'Enyi mifupa mikavu, lisikieni
neno la Yehova:

5 "'Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova ameiambia mifupa hii hivi: "Tazama, ninaleta
ndani yenu pumzi, nanyi lazima muwe hai.[c] **6** Nami nitaweka juu yenu kano na kufanya nyama ije juu yenu, nami
nitaitandaza ngozi juu yenu na
kutia pumzi ndani yenu, nanyi
mtakuwa hai;[d] nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni
Yehova."'"[e]

7 Nami nikatoa unabii kama
nilivyoamriwa.[f] Na sauti ikaanza kutokea mara tu nilipotoa unabii, na tazama, kulikuwa na sauti ya kugongana,
nayo mifupa ikaanza kukaribiana, mfupa kwa mfupa wake.
8 Nami nikaona, na, tazama!
kano na nyama zikaja juu yake
na ngozi ikaanza kutandazwa
juu yake. Lakini kwa habari
ya pumzi, hamkuwa na yoyote
ndani yake.

9 Naye akaendelea kuniambia: "Tolea upepo unabii. Toa
unabii, Ee mwana wa binadamu, nawe utauambia upepo,
'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Ingia kutoka kwenye zile pepo nne, Ee
upepo, na upulize juu ya watu
hawa waliouawa,[g] ili wawe
hai."'"[h]

SURA 36
a Zek 8:8
b Isa 58:12
Yer 33:10
Amo 9:14
c 2Nya 36:21
Yer 25:9
d Mwa 2:8
Mwa 13:10
e Isa 51:3
f Eze 17:24
Eze 37:28
g Hes 23:19
Eze 22:14
Eze 28:26
Eze 37:14
h Zb 102:17
Isa 55:6
Yer 29:12
Yer 50:5
Zek 13:9
Mt 7:7
i Eze 36:10
j Kut 23:17
2Nya 7:8
k Yer 30:19
Yer 31:27

SURA 37
l Eze 1:3
m Eze 3:14
Ufu 21:10
n Ufu 11:9

Safu ya 2
a Eze 37:11
b Kum 32:39
1Sa 2:6
Ro 4:17
2Ko 1:9
c Mwa 2:7
Zb 104:30
Eze 37:14
d Ufu 11:11
e Yoe 2:27
f Eze 37:10
g Ufu 11:7
h Zb 104:30

10 Nami nikatoa unabii
kama vile alivyokuwa ameniamuru, nayo pumzi ikaanza kuingia ndani yao, nao wakaanza
kuishi na kusimama kwa miguu yao,[a] jeshi kubwa, naam,
kubwa sana.
11 Naye akaendelea kuniambia: "Mwana wa binadamu, kwa habari ya mifupa hii,
hii ni nyumba nzima ya Israeli.[b] Tazama, wanasema, 'Mifupa yetu imekauka, nalo tumaini letu limeangamia.[c] Tumekatiliwa mbali, tukabaki peke
yetu.' **12** Kwa hiyo toa unabii, nawe utawaambia, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Tazama ninayafungua makaburi yenu,[d]
nami nitawatoa kutoka katika makaburi yenu, enyi watu
wangu, na kuwaingiza katika nchi ya Israeli.[e] **13** Nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova nitakapoyafungua makaburi yenu
na nitakapowatoa ninyi kutoka katika makaburi yenu, enyi
watu wangu."'[f] **14** 'Nami nitaitia roho yangu ndani yenu,
nanyi mtakuwa hai,[g] nami nitawakalisha katika nchi yenu;
nanyi mtalazimika kujua kwamba mimi mwenyewe, Yehova,
nimesema nami nimelifanya,' asema Yehova."[h]
15 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **16** "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, jichukulie kijiti[i] na uandike juu
yake, 'Kwa Yuda na kwa wenzake, wana wa Israeli.'[j] Na
uchukue kijiti kingine na kuandika juu yake, 'Kwa Yosefu, kijiti cha Efraimu,[k] na wenzake, nyumba yote ya Israeli.'[a] **17** Na uvifanye vikaribiane viwe kijiti kimoja kwa ajili
yako mwenyewe, navyo kwa kweli vitakuwa kimoja tu mkononi mwako.[b] **18** Na wana wa watu wako watakapoanza
kukuambia, 'Je, hutatuambia mambo haya yana maana gani
kwako?'[c] **19** waambie, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Tazama, ninakichukua kijiti cha Yosefu,
kilicho mkononi mwa Efraimu, na wenzake, makabila ya
Israeli, nami nitawaweka juu yake, yaani, kijiti cha Yuda,
nami kwa kweli nitavifanya kuwa kijiti kimoja,[d] navyo vitakuwa kimoja mkononi mwangu."' **20** Navyo vijiti utakavyoandika juu yake vitakuwa mkononi mwako mbele ya
macho yao.[e]
21 "Nawe uwaambie, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Tazama, ninawachukua wana wa Israeli kutoka katikati ya mataifa ambako wameenda, nami
nitawakusanya kutoka pande zote na kuwaleta katika nchi
yao.[f] **22** Nami kwa kweli nitawafanya kuwa taifa moja katika nchi hiyo,[g] kwenye milima ya Israeli, na mfalme mmoja atakuwa mfalme wao wote,[h]
nao hawataendelea tena kuwa mataifa mawili, wala hawataendelea tena kugawanyika katika falme mbili.[i] **23** Nao
hawatajitia unajisi tena kwa sanamu zao za mavi na kwa
machukizo yao na kwa makosa yao yote;[j] nami hakika nitawaokoa kutoka katika makao yao yote ambamo wametenda dhambi ndani yake, nami

SURA 37
a Ufu 11:11
b Eze 36:10
c Zb 141:7
Isa 49:14
d Isa 66:14
Ufu 11:11
e Eze 11:17
Eze 20:42
Eze 36:24
Amo 9:14
f Zb 126:2
Eze 37:6
g Isa 32:15
Eze 36:27
Eze 37:5
h Hes 23:19
Eze 36:36
i Hes 17:2
Eze 37:19
j 2Nya 15:9
2Nya 30:11
k 1Fa 12:20

Safu ya 2
a 1Fa 11:31
b Isa 11:13
Yer 3:18
Yer 50:4
c Eze 12:9
d Yer 50:4
Zek 10:6
e Eze 12:3
f Kum 30:3
Isa 11:12
Yer 16:15
Yer 23:3
Amo 9:14
g Yer 3:18
Ho 1:11
h Mwa 49:10
Zb 2:6
Isa 9:6
Yer 23:5
Lu 1:32
i Eze 37:16
Zek 10:6
j Isa 2:18
Eze 11:18
Eze 20:43
Ho 14:8
Zek 13:2

nitawasafisha,[a] nao watakuwa watu wangu, na mimi mwenyewe nitakuwa Mungu wao.[b]

24 “‘“Na mtumishi wangu Daudi atakuwa mfalme juu yao,[c] nao wote watakuwa na mchungaji mmoja;[d] nao watatembea katika maamuzi yangu ya hukumu,[e] na sheria zangu watazishika,[f] nao hakika watazifanya.[g] **25** Nao kwa kweli watakaa juu ya nchi niliyompa mtumishi wangu, Yakobo, ambamo mababu zenu walikaa,[h] nao kwa kweli watakaa juu yake,[i] wao na wana wao na wana wa wana wao mpaka wakati usio na kipimo,[j] na Daudi mtumishi wangu atakuwa mkuu wao mpaka wakati usio na kipimo.[k]

26 “‘“Nami nitafanya agano la amani[l] pamoja nao; watakuwa na agano lenye kudumu mpaka wakati usio na kipimo.[m] Nami nitawaweka na kuwazidisha[n] na kuweka patakatifu pangu katikati yao mpaka wakati usio na kipimo.[o] **27** Na maskani yangu kwa kweli itakuwa juu yao,[p] nami hakika nitakuwa Mungu wao, na wao wenyewe watakuwa watu wangu.[q] **28** Na mataifa watalazimika kujua kwamba mimi, Yehova,[r] ninawatakasa Israeli wakati patakatifu pangu patakapokuwa katikati yao mpaka wakati usio na kipimo.”’”[s]

38 Nalo neno la Yehova likaendelea kunijia, na kusema: **2** “Mwana wa binadamu,[t] elekeza uso wako juu ya Gogu wa nchi ya Magogu,[u] mkuu wa wakuu wa Mesheki[v] na Tubali,[w] na utoe unabii juu yake. **3** Nawe utasema, ‘Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: “Tazama, niko dhidi yako, Ee Gogu, wewe mkuu wa wakuu wa Mesheki na Tubali. **4** Nami hakika nitakugeuza na kutia kulabu katika mataya yako[a] na kukutoa pamoja na jeshi lako lote,[b] farasi na wapanda-farasi, wote wakiwa wamevaa mavazi yenye kupendeza,[c] kutaniko kubwa sana, lenye ngao kubwa na ngao ndogo, wote wakiwa na panga;[d] **5** Uajemi,[e] Ethiopia[f] na Putu[g] pamoja nao, wote wakiwa na ngao ndogo na kofia; **6** Gomeri[h] na vikosi vyake vyote, nyumba ya Togarma,[i] wa sehemu za mbali zaidi za kaskazini, na vikosi vyake vyote, vikundi vingi vya watu pamoja nawe.[j]

7 “‘“Uwe tayari, nawe ujitayarishe, wewe pamoja na kutaniko lako lote,[k] wale waliokutanika kando yako, nawe utakuwa mlinzi wao.

8 “‘“Baada ya siku nyingi utakaziwa fikira. Katika miaka ya mwisho utakuja katika nchi[l] ya watu waliorudishwa kutoka kwenye upanga, waliokusanywa kutoka kwa vikundi vingi vya watu,[m] na kuletwa kwenye milima ya Israeli, ambayo imekuwa mahali palipoharibika daima; naam, nchi ambayo imerudishwa kutoka kwa vikundi vya watu, ambamo wamekaa kwa usalama, hao wote.[n] **9** Nawe lazima utapanda. Utaingia kama dhoruba.[o] Utakuwa kama mawingu ya kuifunika nchi,[p] wewe na vikosi vyako vyote na vikundi vingi vya watu pamoja nawe.”’

SURA 37

a Law 20:7
b Mwa 17:7; Yer 31:33; Eze 36:28
c Yer 23:5; Yer 30:9; Ho 3:5; Lu 1:32
d Yoh 10:16; 1Pe 5:4
e Zb 25:9
f Kum 30:10
g Yer 32:39; Eze 36:27
h Yer 30:3; Eze 28:25
i Yoe 3:20
j Isa 60:21; Amo 9:15
k Eze 34:24; Lu 1:32; Yoh 12:34
l Eze 34:25
m Isa 55:3; Yer 32:40
n Yer 30:19; Zek 8:5; Ebr 6:14
o Law 26:11; 2Ko 6:16
p Ufu 21:3
q Law 26:12; Eze 11:20; Eze 36:28; Eze 43:7; Ho 2:23
r Eze 36:23
s Eze 20:12

SURA 38

t Eze 39:1
u Eze 38:15; Eze 39:6
v Eze 32:26
w Isa 66:19; Eze 27:13

Safu ya 2

a 2Fa 19:28; Eze 29:4; Eze 39:2
b Eze 38:15
c Eze 23:12
d Yer 46:9
e Eze 27:10
f Eze 30:5
g 1Nya 1:8
h Mwa 10:2
i Mwa 10:3; Eze 27:14
j Eze 39:2
k Isa 8:9; Yer 46:3; Yoe 3:9
l Isa 66:8
m Mt 24:31
n Yer 23:6; Eze 28:26; Eze 34:25
o Isa 28:2
p Yer 4:13

10 "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Na itatukia katika siku hiyo kwamba mambo yataingia moyoni mwako,[a] nawe hakika utapanga hila yenye madhara;[b] **11** nawe utasema: "Nitapanda juu ya nchi iliyo wazi ya mashambani.[c] Nitawaingilia wale wasio na usumbufu, wanaokaa kwa usalama, wote wanaokaa bila ukuta,[d] nao hawana hata mapingo na milango." **12** Ili kuteka nyara kubwa na kupora kwa wingi,[e] ili kuugeuzia mkono wako kuelekea mahali palipoharibiwa panapokaliwa tena[f] na juu ya kikundi cha watu waliokusanywa pamoja kutoka katika mataifa,[g] wanaokusanya utajiri na mali,[h] wale wanaokaa katikati[i] ya dunia.

13 "'Sheba[j] na Dedani[k] na wanabiashara wa Tarshishi[l] na wana-simba wake wote wenye manyoya shingoni[m]—hao watakuambia: "Je, unakuja kuteka nyara kubwa? Je, umekutanisha kutaniko lako ili kupora kwa wingi, ili kuchukua fedha na dhahabu, kuchukua utajiri na mali, ili kuteka nyara kubwa sana?"'

14 "Kwa hiyo toa unabii, Ee mwana wa binadamu, nawe umwambie Gogu, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Je, haitakuwa katika siku ile wakati watu wangu Israeli wanapokaa kwa usalama kwamba utajua hilo?[n] **15** Nawe hakika utakuja kutoka mahali pako, kutoka sehemu za mbali zaidi za kaskazini,[o] wewe na vikundi vingi vya watu pamoja nawe, hao wote wakiwa wamepanda farasi, kutaniko kubwa, naam, jeshi kubwa sana.[a] **16** Nawe utalazimika kupanda na kuja juu ya watu wangu Israeli, kama mawingu ili kuifunika nchi.[b] Itatukia katika siku za mwisho, nami hakika nitakuleta wewe juu ya nchi yangu,[c] kusudi mataifa yanijue mimi wakati ninapojitakasa mwenyewe kupitia kwako mbele ya macho yao, Ee Gogu."'[d]

17 "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Je, wewe ndiye[e] yuleyule niliyesema juu yake katika siku za zamani kwa mkono wa watumishi wangu hao manabii wa Israeli, waliokuwa wakitoa unabii katika siku hizo—miaka—juu ya kukuleta wewe juu yao?'[f]

18 "'Na itatukia katika siku hiyo, katika siku ambayo Gogu atakuja juu ya nchi ya Israeli,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'kwamba ghadhabu yangu itapanda puani mwangu.[g] **19** Na katika ukali wangu,[h] katika moto wa ghadhabu yangu, nitalazimika kusema.[i] Kwa kweli katika siku hiyo tetemeko kubwa litatukia katika nchi ya Israeli.[j] **20** Na kwa sababu yangu samaki wa baharini na viumbe vinavyoruka vya mbinguni na wanyama wa mwituni na vitu vyote vinavyotambaa juu ya nchi na wanadamu wote walio katika uso wa nchi watalazimika kutetemeka,[k] nayo milima kwa kweli itaangushwa chini[l] na njia zenye mwinuko mkali zitaanguka, na kila ukuta utaanguka chini.'

21 "'Nami nitaita upanga juu yake kotekote katika eneo la-

SURA 38

a Zb 83:4
b Met 6:18; Ufu 17:13
c Kut 15:9; Yer 49:31
d Isa 26:1; Zek 2:4
e Met 1:13
f Yer 33:12
g Zek 10:8
h Isa 60:5; Isa 61:6
i Zek 2:8
j Eze 27:22
k Eze 27:15
l Eze 27:25
m Yer 50:17
n Eze 38:8
o Eze 39:2

Safu ya 2

a Sef 3:8
b Eze 38:9
c Yoe 3:2
d Kut 14:4; 2Fa 19:19; Zb 83:18; Zb 148:14; Eze 36:23; Eze 39:21; Mt 6:9
e Kut 9:16; Isa 14:12; Yer 50:31; Eze 28:17
f Yoe 3:16; Zek 2:8
g Kum 32:22; Nah 1:2; Ebr 12:29
h Zb 78:21
i Ebr 12:29
j Hab 3:6
k Ho 4:3
l Yer 4:24; Nah 1:5

ngu lote lenye milima,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.[a] 'Upanga wa kila mmoja utakuwa juu ya ndugu yake.[b] **22** Nami nitajiingiza mwenyewe katika hukumu[c] pamoja naye, kwa tauni[d] na kwa damu;[e] nami nitanyesha mvua kubwa yenye kufurika na mawe,[f] moto[g] na kiberiti juu yake na juu ya vikosi vyake na juu ya vikundi vingi vya watu vitakavyokuwa pamoja naye.[h] **23** Nami hakika nitajitukuza mwenyewe na kujitakasa mwenyewe[i] na kujijulisha mwenyewe mbele ya macho ya mataifa mengi; nao watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova.'[j]

39 "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, toa unabii juu ya Gogu,[k] nawe useme, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Tazama niko dhidi yako, Ee Gogu, ewe mkuu wa wakuu wa Mesheki[l] na Tubali.[m] **2** Nami nitakugeuza na kukuongoza[n] na kukufanya uje kutoka katika sehemu za mbali zaidi za kaskazini[o] na kukuingiza kwenye milima ya Israeli. **3** Nami nitaupiga upinde wako utoke katika mkono wako wa kushoto, nayo mishale yako nitaiangusha kutoka katika mkono wako mwenyewe wa kuume. **4** Utaanguka juu ya milima ya Israeli,[p] wewe na vikosi vyako vyote na vikundi vya watu vitakavyokuwa pamoja nawe. Nitakutoa uwe chakula cha ndege wenye kuwinda, na ndege wa kila namna ya bawa, na wanyama wa mwituni."'[q]

5 "'Utaanguka juu ya uso wa nchi,[r] kwa maana mimi mwenyewe nimesema,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

6 "'Nami nitatuma moto juu ya Magogu[a] na juu ya wale wanaokaa visiwani kwa usalama;[b] na watu watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova. **7** Na jina langu takatifu nitalijulisha katikati ya watu wangu Israeli, wala sitaliacha tena jina langu litiwe unajisi;[c] na mataifa watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova,[d] Mtakatifu katika Israeli.'[e]

8 "'Tazama! itakuwa na lazima itatendeka,'[f] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. 'Hii ndiyo siku ambayo nimesema juu yake.[g] **9** Na wakaaji wa majiji ya Israeli hakika wataenda na kuteketeza na kuwasha mioto kwa silaha na ngao ndogo na ngao kubwa, —kwa pinde na kwa mishale na kwa fimbo na kwa mikuki; nao watazitumia kuwasha mioto[h] kwa miaka saba. **10** Nao hawatachukua vijiti shambani, wala hawatakusanya kuni misituni, kwa maana watatumia silaha kuwasha mioto.'

"'Nao hakika watawateka nyara wale waliokuwa wakiwateka nyara,[i] na kuwapora wale waliokuwa wakiwapora,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

11 "'Na itatukia kwamba katika siku hiyo, nitampa Gogu[j] mahali huko, kaburi katika Israeli, bonde la wale wanaopita katikati upande wa mashariki wa bahari, nalo litakuwa likiwazuia wale wanaopita katikati. Nao watalazimika kumzika Gogu na umati wake wote huko, nao hakika

SURA 38
a Eze 14:17
b 2Nya 20:23 Hag 2:22 Zek 14:13
c Yer 25:31
d Zek 14:12
e Isa 66:16
f Kut 9:22 Yos 10:11 Zb 18:12
g Isa 29:6 Isa 30:30
h Mwa 19:24 Zb 11:6
i Law 22:32 Eze 36:23
j Zb 9:16 Eze 25:17

SURA 39
k Eze 38:2
l Eze 32:26
m Eze 27:13
n Eze 38:4
o Eze 38:15
p Eze 38:21
q Eze 32:4 Eze 33:27 Ufu 19:18
r Yer 8:2 Yer 25:33

Safu ya 2
a Eze 38:22
b Zb 72:10
c Law 18:21 Eze 20:9
d Eze 38:16
e Isa 6:3
f Ufu 16:17
g Isa 46:10 2Pe 3:10
h Yos 11:6 Zb 46:9
i Ayu 34:11 Isa 14:2 Mt 7:2 Ufu 18:6
j Eze 38:2

wataliita, Bonde la Umati wa Gogu.[a] **12** Na wale wa nyumba ya Israeli watalazimika kuwazika hao ili kuisafisha nchi, kwa miezi saba.[b] **13** Na watu wote wa nchi watalazimika kuzika, na hakika kwao hilo litakuwa jambo lenye sifa katika siku ambayo nitajitukuza mwenyewe,'[c] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

14 "'Na kutakuwa na watu kwa ajili ya kazi ya kuajiriwa yenye kuendelea ambao watawatenga, wakipita katikati ya nchi, wakizika, na wale wanaopita katikati, wale waliobaki kwenye uso wa dunia, ili kuisafisha. Mpaka mwisho wa miezi saba wataendelea kutafuta. **15** Na wale wanaopita katikati lazima wapite nchini, na mtu akiuona mfupa wa mwanadamu ataweka pia alama kando yake, mpaka wale wanaozika watakapokuwa wameuzika katika Bonde la Umati wa Gogu.[d] **16** Nalo jina la jiji hilo litakuwa pia Hamona. Nao watalazimika kuitakasa nchi.'[e]

17 "Na wewe, Ee mwana wa binadamu, Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Sema na ndege wa kila namna ya bawa na wanyama wote wa mwituni:[f] "Kusanyikeni pamoja na mje. Jikusanyeni pamoja pande zote kwenye dhabihu yangu, ambayo ninatoa kwa ajili yenu, dhabihu kubwa juu ya milima ya Israeli.[g] Nanyi hakika mtakula nyama na kunywa damu.[h] **18** Mtakula nyama ya wenye nguvu, nanyi mtakunywa damu ya wakuu wa dunia,[i] kondoo-dume, na wana-kondoo,[j] na mbuzi-dume, ngombe-dume wachanga,[a] vinono wote wa Bashani.[b] **19** Nanyi hakika mtakula mafuta mpaka mshibe[c] na kunywa damu mpaka mlewe, kutokana na dhabihu yangu nitakayotoa kwa ajili yenu."'

20 "'Nanyi mtashiba mezani pangu kwa farasi na waendesha-gari, watu wenye nguvu na mashujaa wa vita wa namna zote,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.[d]

21 "'Nami nitaweka utukufu wangu kati ya mataifa; na mataifa yote yatalazimika kuiona hukumu yangu ambayo nimeitenda[e] na mkono wangu ambao nimeuweka katikati yao.[f] **22** Na wale wa nyumba ya Israeli watalazimika kujua kwamba mimi ni Yehova Mungu wao kuanzia siku hiyo na kuendelea.[g] **23** Nayo mataifa yatalazimika kujua kwamba ilikuwa kwa sababu ya kosa lao kwamba wao, nyumba ya Israeli, walienda uhamishoni,[h] kwa sababu walijiendesha kwa kukosa uaminifu kunielekea mimi, hivi kwamba nikawaficha wao uso wangu[i] na kuwatia mkononi mwa wapinzani wao, nao wakawa wakianguka, wote hao, kwa upanga.[j] **24** Niliwatendea kulingana na uchafu wao na kulingana na ukosaji wao,[k] nami nikaendelea kuwaficha uso wangu.'

25 "Kwa hiyo Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Sasa nitawarudisha mateka wa Yakobo[l] na kwa kweli niwe na rehema juu ya nyumba yote ya Israeli;[m] nami nitajitoa kikamili kwa ajili ya jina langu takatifu.[n] **26** Nao watakuwa wamechukua fe-

SURA 39
a Eze 39:15
b Kum 21:23
c Eze 28:22
Eze 38:16
d Eze 39:11
e Eze 39:12
f Yer 12:9
Sef 1:7
g Isa 34:6
Yer 46:10
Eze 32:4
Ufu 19:17
h Ufu 19:18
i Eze 29:5
j Yer 51:40

Safu ya 2
a Isa 34:7
Yer 50:27
b Kum 32:14
Zb 22:12
Amo 4:1
c Ufu 19:21
d Zb 76:6
Eze 38:4
Hag 2:22
Ufu 19:18
e Kut 14:4
Isa 37:20
Eze 36:23
Eze 38:16
Mal 1:11
f Kut 7:4
Kut 8:19
1Sa 5:7
1Sa 6:9
g Zb 9:16
Yer 24:7
h 2Nya 7:22
Yer 22:9
i Kum 31:18
Zb 30:7
Isa 59:2
j Law 26:25
Kum 32:30
Zb 106:41
k Law 26:24
Eze 36:19
l Yer 30:3
Eze 34:13
m Yer 31:1
Ho 1:11
Zek 1:16
n Kut 34:14
Eze 36:21

dheha[a] yao na ukosefu wao
wote wa uaminifu ambao wa-
menitendea,[b] wakati watakapokaa katika nchi yao kwa
usalama,[c] pasipo mtu yeyote
wa kuwatetemesha.[d] **27** Ni-
takapowarudisha kutoka kati-
ka vikundi vya watu nami kwa
kweli niwakusanye pamoja ku-
toka katika nchi za adui zao,[e]
mimi pia nitajitakasa mwenye-
we katikati yao mbele ya ma-
cho ya mataifa mengi.'[f]

28 "'Nao watalazimika ku-
jua kwamba mimi ni Yehova
Mungu wao, nitakapowapeleka uhamishoni kwa mataifa na
kwa kweli niwarudishe pamoja kwenye nchi yao,[g] hivi kwa-
mba sitamwacha yeyote kati
yao abaki huko.[h] **29** Nami si-
taendelea tena kuwaficha uso
wangu,[i] kwa sababu nitaimimi-
na roho yangu juu ya nyumba
ya Israeli,[j] asema Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova."

40 Katika mwaka wa 25 wa
uhamisho[k] wetu, mwa-
nzoni mwa mwaka, siku ya 10
ya mwezi, katika mwaka wa 14
baada ya jiji kupigwa na kua-
ngushwa,[l] siku hiyohiyo mko-
no wa Yehova ukawa juu ya-
ngu,[m] hivi kwamba akanileta
mahali hapo.[n] **2** Katika mao-
no ya Mungu alinileta katika
nchi ya Israeli na hatua kwa
hatua akaniweka juu ya mlima
mrefu sana,[o] ambao juu yake
palikuwa na kitu kama muu-
ndo wa jiji kuelekea kusini.[p]

3 Naye akanileta huko, na,
tazama! alikuwapo mtu fulani.
Sura yake ilikuwa kama sha-
ba,[q] naye alikuwa na kamba ya
kitani mkononi mwake, na ute-
te wa kupimia,[r] naye alikuwa
amesimama langoni. **4** Naye
mtu huyo akaanza kuniambia:
"Mwana wa binadamu,[a] ona
kwa macho yako, na kwa ma-
sikio yako usikie, na uweke
moyo wako juu ya yote ninayo-
kuonyesha, kwa sababu umele-
twa hapa nipate kukuonyesha.
Itangazie nyumba ya Israeli
kila kitu unachokiona."[b]

5 Na, tazama! kulikuwa na
ukuta nje ya nyumba kuizu-
nguka pande zote. Na katika
mkono wa mtu huyo kuliku-
wa na utete wa kupimia wenye
urefu wa mikono sita, na we-
nye kipimo cha mkono mmoja
na cha upana wa kiganja kimo-
ja. Naye akaanza kupima upa-
na wa kitu kilichojengwa, ute-
te mmoja; na kimo chake, ute-
te mmoja.

6 Kisha akaja katika lango,
ambalo upande wake wa mbe-
le unaelekea mashariki,[c] aka-
panda juu kwa kutumia ngazi
zake. Naye akaanza kupima ki-
zingiti cha lango hilo,[d] upana
wa utete mmoja, na kile kizi-
ngiti kingine, upana wa ute-
te mmoja. **7** Na chumba cha
walinzi kilikuwa na urefu wa
utete mmoja na upana wa ute-
te mmoja, na kati ya vyumba
vya walinzi[e] kulikuwa na kipi-
mo cha mikono mitano; na ki-
zingiti cha lango kando ya uku-
mbi wa lango kuelekea upa-
nde wa ndani kilikuwa utete
mmoja.

8 Naye akapima ukumbi wa
lango kuelekea upande wa nda-
ni, utete mmoja.[f] **9** Kwa hiyo
akapima ukumbi wa lango, mi-
kono minane; na nguzo zake za
kando, mikono miwili; na uku-
mbi wa lango ulielekea upande
wa ndani.

SURA 39
a Da 9:16
b Zb 99:8
c Law 26:5
d Yer 23:6
e Yer 30:10
Yer 46:27
Eze 28:25
Amo 9:14
Sef 3:20
f Isa 5:16
Eze 36:23
Eze 38:16
g Eze 34:30
h Kum 30:4
i Isa 45:17
Isa 54:8
Yer 29:14
j Isa 32:15
Yoe 2:28
Zek 12:10

SURA 40
k 2Fa 24:15
l 2Fa 25:9
2Nya 36:19
Eze 33:21
m Eze 1:3
n Eze 8:3
o Isa 2:2
Mik 4:1
p Ufu 21:10
q Eze 1:7
Da 10:6
r Zb 78:55
Eze 47:3
Zek 2:1
Ufu 11:1
Ufu 21:15

Safu ya 2
a Eze 44:5
b Yer 26:2
Eze 43:10
Mdo 20:27
c Eze 40:10
Eze 43:1
d Eze 46:2
e 1Nya 9:26
f Eze 40:5

10 Na vyumba vya walinzi vya lango kuelekea mashariki vilikuwa vitatu upande huu na vitatu upande ule. Hivyo vitatu vilikuwa na kipimo kilekile, nazo nguzo za kando zilikuwa na kipimo kilekile, upande huu na upande ule.

11 Kisha akapima upana wa mwingilio wa lango, mikono kumi; urefu wa lango, mikono kumi na mitatu.

12 Na eneo lililozungushiwa ua mbele ya vyumba vya walinzi lilikuwa mkono mmoja, na kulikuwa na eneo la mkono mmoja kila upande lililozungushiwa ua. Na chumba cha mlinzi kilikuwa mikono sita upande huu na mikono sita upande ule.

13 Naye akapima lango kutoka kwenye dari ya chumba kimoja cha mlinzi mpaka kwenye dari ya kile kingine, upana wa mikono 25;[a] mwingilio mmoja ulielekeana na mwingilio mwingine. **14** Kisha akafanya nguzo za kando za mikono 60, pia nguzo za kando za ua katika malango kuzunguka pande zote. **15** Na upande wa mbele wa lango la njia ya kuingilia mpaka upande wa mbele wa ukumbi wa lango la ndani ulikuwa mikono 50.

16 Na palikuwa na madirisha yenye viunzi vyenye upana tofauti[b] kwa ajili ya vyumba vya walinzi na kwa ajili ya nguzo zao za kando kuelekea upande wa ndani wa lango kuzunguka pande zote, na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa ajili ya zile kumbi. Nayo madirisha yalikuwa yenye kuzunguka pande zote kuelekea upande wa ndani, na kwenye nguzo za kando palikuwa na maumbo ya mitende.[a]

17 Naye akanileta hatua kwa hatua ndani ya ua wa nje, na, tazama! palikuwa na vyumba vya kulia chakula,[b] na sakafu ya mawe iliyofanywa kwa ajili ya ua kuzunguka pande zote. Palikuwa na vyumba 30 vya kulia chakula juu ya ile sakafu ya mawe.[c] **18** Nayo sakafu ya mawe kando ya malango ilikuwa sawa kabisa na urefu wa malango—ile sakafu ya chini ya mawe.

19 Naye akapima upana kutoka upande wa mbele wa lango la chini mpaka mbele ya ua wa ndani. Upande wake wa nje ulikuwa mikono mia moja, upande wa mashariki na upande wa kaskazini.

20 Na ua wa nje ulikuwa na lango ambalo upande wake wa mbele ulielekea kaskazini. Akapima urefu wake na upana wake. **21** Navyo vyumba vyake vya walinzi vilikuwa vitatu upande huu na vitatu upande ule. Na nguzo zake za kando na ukumbi wake zilikuwa kulingana na kipimo cha lango la kwanza. Urefu wake mikono 50, na upana wake mikono 25. **22** Na kipimo cha madirisha yake na ukumbi wake na maumbo yake ya mitende[d] kilikuwa sawa na kipimo cha lango ambalo upande wake wa mbele unaelekea mashariki. Na kwa kutumia vipandio saba watu wangeweza kupanda kuingia ndani yake, na ukumbi wake ulikuwa mbele yake.

23 Na lango la ua wa ndani lilielekeana na lango la upande

SURA 40
a Eze 40:21
b 1Fa 6:4
Eze 41:26

Safu ya 2
a 1Fa 6:35
b 1Nya 28:12
c Eze 45:5
d Eze 41:20
Eze 41:26

wa kaskazini; pia lile la upande
wa mashariki. Naye akapima
kutoka lango moja mpaka la-
ngo lingine mikono mia moja.
24 Naye akanileta hatua kwa
hatua upande wa kusini,[a]
na, tazama! kulikuwa na lango
upande wa kusini, naye akapi-
ma nguzo zake za kando na uku-
mbi wake kwa vipimo sawa na
hivi. **25** Na palikuwa na madi-
risha kuzunguka pande zote juu
yake na juu ya ukumbi wake,
kama madirisha hayo. Urefu
wake mikono 50, na upana wake
mikono 25. **26** Na palikuwa
na ngazi saba za kulipandia,
na ukumbi wake ulikuwa mbele
yake.[b] Nalo lilikuwa na maumbo
ya mitende, moja upande huu na
lingine upande ule juu ya nguzo
zake za kando.
27 Na ua wa ndani uliku-
wa na lango upande wa kusi-
ni. Naye akapima kutoka lango
mpaka lango upande wa kusi-
ni mikono mia moja. **28** Naye
akanileta hatua kwa hatua
mpaka ndani ya ua wa ndani
kupitia lango la kusini. Naye
akalipima lango la kusini kwa
vipimo sawa na hivi. **29** Na-
vyo vyumba vyake vya wali-
nzi na nguzo zake za kando
na ukumbi wake vilikuwa na
vipimo sawa na hivi. Na pali-
kuwa na madirisha kuzungu-
ka pande zote juu yake na juu
ya ukumbi wake. Urefu wake
mikono 50, na upana wake mi-
kono 25.[c] **30** Na palikuwa na
kumbi kuzunguka pande zote;
urefu wake mikono 25, na
upana wake mikono 5. **31** Na
ukumbi wake ulielekea ua wa
nje, na maumbo ya mitende
yalikuwa kwenye nguzo zake

SURA 40
a Eze 46:9
b Eze 40:22
c Eze 40:21

za kando,[a] na mpando wake uli-
kuwa vipandio vinane.[b]
32 Naye akanileta hatua
kwa hatua ndani ya ua wa nda-
ni kupitia njia ya mashariki,
naye akapima lango kwa vipi-
mo sawa na hivi. **33** Navyo
vyumba vyake vya walinzi na
nguzo zake za kando na uku-
mbi wake vilikuwa na vipi-
mo sawa na hivi, hilo na uku-
mbi wake lilikuwa na madiri-
sha kuzunguka pande zote juu.
Urefu wake mikono 50, na upa-
na wake mikono 25. **34** Na
ukumbi wake ulielekea ua wa
nje, na maumbo ya mitende
yalikuwa kwenye nguzo zake
za kando upande huu na upa-
nde ule. Na mpando wake uli-
kuwa vipandio vinane.
35 Naye akanileta ndani ya
lango la kaskazini,[c] naye akapi-
ma, kwa vipimo sawa na hivi,[d]
36 vyumba vyake vya walinzi,
nguzo zake za kando na uku-
mbi wake. Nalo lilikuwa na ma-
dirisha kuzunguka pande zote.
Urefu wake mikono 50, na upa-
na wake mikono 25. **37** Na
kuelekea ua wake wa nje pali-
kuwa na nguzo zake za kando,
na maumbo ya mitende yaliku-
wa juu ya nguzo zake za kando
upande huu na upande ule.[e]
Na mpando wake ulikuwa vi-
pandio vinane.
38 Na chumba cha kulia
chakula pamoja na mwingilio
wake kilikuwa kando ya ngu-
zo za kando za malango. Hapo
ndipo walipokuwa wakioshea
toleo zima la kuteketezwa.[f]
39 Na katika ukumbi wa la-
ngo palikuwa na meza mbili
upande huu na meza mbili upa-
nde ule, za kuchinjia juu yake

Safu ya 2
a Eze 40:16
b Eze 40:34
Eze 40:37
c Eze 44:4
d Eze 40:32
e Eze 40:31
f Law 8:21

lile toleo zima la kuteketezwa[a] na lile toleo la dhambi[b] na lile toleo la hatia.[c] **40** Na upande wa nje, mtu anapopanda mpaka kwenye mwingilio wa lango la kaskazini, palikuwa na meza mbili. Na ule upande mwingine wa ukumbi wa lango palikuwa na meza mbili. **41** Palikuwa na meza nne hapa na meza nne pale kando ya lango—meza nane, ambazo walikuwa wakichinjia juu yake. **42** Na zile meza nne kwa ajili ya toleo zima la kuteketezwa zilikuwa za mawe yaliyochongwa. Urefu wake mkono mmoja na nusu, na upana wake mkono mmoja na nusu, na kimo kilikuwa mkono mmoja. Juu yake pia walikuwa wakiweka vifaa ambavyo walikuwa wakitumia kuchinjia toleo zima la kuteketezwa na ile dhabihu. **43** Na rafu za kuwekea vitu zilikuwa na upana wa kiganja kimoja, zikiwa zimefungwa kwa uthabiti upande wa ndani, kuzunguka pande zote; na juu ya meza walikuwa wakiweka nyama ya toleo la zawadi.[d]

44 Na upande wa nje wa lango la ndani palikuwa na vyumba vya kulia chakula vya waimbaji,[e] katika ua wa ndani, ulio upande wa lango la kaskazini. Na upande wake wa mbele ulielekea kusini. Palikuwa na kimoja upande wa lango la mashariki. Upande wake wa mbele ulielekea kaskazini.

45 Naye akaniambia: "Hiki, chumba cha kulia chakula ambacho upande wake wa mbele unaelekea kusini, ni cha makuhani wanaotimiza wajibu wa nyumba.[f] **46** Na chumba cha kulia chakula ambacho upande wake wa mbele unaelekea kaskazini ni cha makuhani wanaotimiza wajibu wa madhabahu.[a] Hao ni wana wa Sadoki,[b] ambao, kutoka kwa wana wa Lawi, wanamkaribia Yehova ili kumhudumia."[c]

47 Naye akapima ua wa ndani. Urefu wake ulikuwa mikono 100, na upana mikono 100, mraba. Nayo madhabahu ilikuwa mbele ya nyumba.

48 Naye akanileta ndani ya ukumbi wa nyumba, naye akapima nguzo ya kando ya ukumbi,[d] mikono 5 upande huu na mikono 5 upande ule. Na upana wa lango ulikuwa mikono 3 upande huu na mikono 3 upande ule.

49 Urefu wa ukumbi ulikuwa mikono 20, na upana wake mikono 11. Nao walikuwa wakiupanda kwa kutumia ngazi. Na palikuwa na nguzo kando ya miimo ya kando, mmoja hapa na mmoja pale.[e]

41 Naye akanileta hekaluni, akapima zile nguzo za kando, mikono 6 upana wake hapa na mikono 6 upana wake pale, upana wa nguzo ya kando. **2** Nao upana wa mwingilio ulikuwa mikono 10, na sehemu za kando za mwingilio zilikuwa mikono 5 hapa na mikono mitano pale. Naye akapima urefu wake, mikono 40; na upana, mikono 20.

3 Naye akaingia ndani na kupima nguzo ya kando ya mwingilio, mikono 2; na mwingilio, mikono 6; na upana wa mwingilio ulikuwa mikono 7. **4** Naye akapima urefu wake, mikono 20; na upana wake, miko-

SURA 40

a Law 1:3
Eze 43:18

b Law 4:3

c Law 5:6
Law 7:1
Eze 42:13
Eze 44:29

d Law 1:6
Law 8:20

e 1Nya 6:31
Efe 5:19
Kol 3:16

f Law 8:35
Hes 3:7
Hes 3:32
1Nya 9:23
2Nya 13:11
Zb 134:1

Safu ya 2

a Law 6:12
Hes 18:5

b 1Fa 2:35
Eze 43:19

c Hes 16:40
Eze 44:15

d 1Fa 6:3
2Nya 3:4

e 1Fa 7:21
Yer 52:17
Ufu 3:12

no 20,[a] mbele ya hekalu. Kisha akaniambia: "Hapa ndipo Patakatifu Zaidi."[b]

5 Naye akapima ukuta wa nyumba, mikono sita. Na upana wa chumba cha kando ulikuwa mikono minne, kuzunguka pande zote; uliizunguka nyumba yote pande zote.[c] **6** Navyo vyumba vya kando vilikuwa chumba cha kando juu ya chumba cha kando, ghorofa tatu, na kila sehemu ikiwa na 30; navyo viliingia ndani ya ukuta wa nyumba, yaani, vyumba vya kando kuzunguka pande zote, ili vipate kushikiliwa, lakini havikushikiliwa katika ukuta wa nyumba.[d] **7** Navyo vilipanuka kuelekea upande wa nje na kugeuka kuelekea sehemu ya juu na ile iliyo juu yake mpaka kwenye vile vyumba vya kando, kwa maana njia inayopinda-pinda ya nyumba ile ilienda juu na juu kuizunguka nyumba pande zote.[e] Kwa hiyo nyumba ilipanuka kuelekea juu, na kutoka ghorofa ya chini kabisa mtu angeweza kupanda mpaka ghorofa ya juu kabisa,[f] kupitia ghorofa ya katikati.

8 Nami nikaona kwamba kulikuwa na jukwaa refu kwa ajili ya nyumba kuizunguka pande zote. Nayo misingi ya nguzo za kando, ilikuwa utete mzima wa mikono sita mpaka kwenye mahali pa kuungania.[g] **9** Upana wa ukuta uliokuwa wa chumba cha kando, upande wa nje, ulikuwa mikono mitano. Na kulikuwa na nafasi iliyoachwa wazi kwa ujenzi wa vyumba vya kando vilivyokuwa vya nyumba hiyo.

SURA 41
a 1Fa 6:20 2Nya 3:8
b Kut 26:33
c 1Fa 6:5
d 1Fa 6:6 1Fa 6:10
e 1Fa 6:8
f Eze 42:5
g Eze 40:5

10 Na kati ya vile vyumba vya kulia chakula[a] upana ulikuwa mikono 20 kuizunguka nyumba, pande zote. **11** Nao mwingilio wa chumba cha kando ulikuwa katika upande wa ile nafasi iliyoachwa wazi, mwingilio mmoja ukielekea kaskazini na mwingilio mmoja upande wa kusini; nao upana wa eneo la nafasi iliyoachwa wazi ulikuwa mikono mitano, kuzunguka pande zote.

12 Nalo jengo lililokuwa mbele ya eneo lililotengwa, ambalo upande wake wa kando ulielekea magharibi, lilikuwa na upana wa mikono 70. Nao ukuta wa jengo ulikuwa na upana wa mikono 5, kuzunguka pande zote; nao urefu wake ulikuwa mikono 90.

13 Naye akaipima nyumba, mikono mia moja urefu wake; na lile eneo lililotengwa na jengo na kuta zake, mikono mia moja urefu wake. **14** Nao upana wa upande wa mbele wa nyumba na lile eneo lililotengwa katika upande wa mashariki ulikuwa mikono mia moja.

15 Naye akapima urefu wa jengo mbele ya lile eneo lililotengwa lililokuwa nyuma yake na mabaraza yake upande huu na upande ule, mikono mia moja.

Pia hekalu na mahali pa ndani zaidi[b] na zile kumbi za ua; **16** vizingiti, na madirisha yenye viunzi vyenye upana tofauti,[c] na mabaraza yalizunguka hizo tatu pande zote. Mbele ya kizingiti kulikuwa na mbao zilizofunika kuzunguka pande zote,[d] na kutoka kwenye sakafu mpaka madirishani; nayo

Safu ya 2
a 1Nya 28:12
b 2Nya 3:8 Eze 41:4
c 1Fa 6:4
d 1Fa 6:15 2Nya 3:5

madirisha yalikuwa yamefunikwa. **17** Mpaka juu ya mwingilio na kufikia nyumba ya ndani na upande wa nje na juu ya ukuta wote kuzunguka pande zote, kwenye nyumba ya ndani na nje, kulikuwa na vipimo, **18** hata makerubi[a] waliochongwa na maumbo ya mitende,[b] pakiwa umbo la mtende katikati ya kerubi na kerubi, naye kerubi alikuwa na nyuso mbili.[c] **19** Nao uso wa mwanadamu ulielekea umbo la mtende upande huu, na uso wa mwana-simba mwenye manyoya shingoni ulielekea umbo la mtende upande ule,[d] wakiwa wamechongwa juu ya nyumba yote kuizunguka pande zote. **20** Kutoka sakafuni mpaka juu ya mwingilio kulikuwa na makerubi waliochongwa na maumbo ya mitende, kwenye ukuta wa hekalu.

21 Kwa habari ya hekalu, miimo ya mlango ilikuwa mraba;[e] na mbele ya mahali patakatifu kulikuwa na sura kama sura ifuatayo: **22** ile madhabahu ya mbao ilikuwa na kimo cha mikono mitatu, nao urefu wake ulikuwa mikono miwili, nayo ilikuwa na miimo yake ya pembeni.[f] Nao urefu wake na kuta zake zilikuwa za mbao. Naye akaniambia: "Hii ndiyo meza iliyo mbele za Yehova."[g]

23 Nalo hekalu na mahali patakatifu palikuwa na milango miwili.[h] **24** Na sehemu mbili za mlango zilikuwa kwenye milango, hizo mbili zikiwa zenye kukunjika. Mlango mmoja ulikuwa na sehemu mbili za mlango zenye kukunjika, na ule mlango mwingine ulikuwa na sehemu mbili za mlango zenye kukunjika. **25** Na juu yake, juu ya milango ya hekalu, palifanyizwa makerubi na maumbo ya mitende,[a] kama ilivyofanywa juu ya kuta, na kulikuwa na kipaa cha mbao juu ya upande wa mbele wa ukumbi upande wa nje. **26** Na kulikuwa na madirisha yenye kiunzi chenye upana tofauti[b] na maumbo ya mitende upande huu na upande ule kandokando ya kumbi za kando na vyumba vya kando vya nyumba na vile vipaa.

42 Naye akanileta hatua kwa hatua[c] mpaka kwenye ua wa nje katika njia inayoelekea kaskazini.[d] Naye akanileta kwenye jengo la chumba cha kulia chakula[e] lililokuwa mbele ya eneo lililotengwa[f] na ambalo lilikuwa mbele ya jengo lililoelekea kaskazini. **2** Mbele ya urefu wa mikono 100 kulikuwa na mwingilio wa kaskazini, nao upana ulikuwa mikono 50. **3** Mbele ya ile mikono 20 iliyokuwa ya ua wa ndani[g] na mbele ya sakafu ya mawe[h] iliyokuwa ya ua wa nje kulikuwa na baraza[i] lenye kuangaliana na baraza katika ghorofa tatu. **4** Na mbele ya vyumba vya kulia chakula palikuwa na njia yenye upana wa mikono kumi kuelekea ndani,[j] njia ya mkono mmoja, nayo miingilio yake ilielekea kaskazini. **5** Na kwa habari ya vyumba vya kulia chakula, vya juu zaidi vilikuwa vifupi, kwa maana yale mabaraza yalivipunguza, kuliko yalivyopunguza vile vya chini zaidi na kuliko yalivyopunguza vile vya katikati, katika jengo

SURA 41
a 1Fa 6:29; 1Fa 7:36; 2Nya 3:7
b Eze 40:16
c Eze 10:14
d Eze 1:10; Ufu 4:7
e 1Fa 6:33
f Kut 30:1; 1Fa 7:48; 2Nya 4:19; Ufu 8:3
g Eze 44:16; Mal 1:7
h 1Fa 6:32; 2Nya 4:22

Safu ya 2
a Eze 41:18
b Eze 40:16

SURA 42
c Eze 40:2; Eze 41:1
d Eze 40:20; Ufu 11:2
e Eze 42:13
f Eze 41:12; Eze 41:15
g Eze 41:10
h 2Nya 7:3; Eze 40:18
i Eze 41:16
j Eze 42:11

hilo. **6** Kwa maana yalikuwa katika ghorofa tatu,[a] nayo hayakuwa na nguzo kama nguzo za zile nyua. Ndiyo sababu sehemu kubwa zaidi ilipunguzwa katika vile vya chini zaidi na katika vile vya katikati kutoka ukutani.

7 Nao ukuta wa mawe uliokuwa nje ulikuwa karibu na vyumba vya kulia chakula kuelekea ua wa nje mbele ya vile vyumba vingine vya kulia chakula. Urefu wake ulikuwa mikono 50. **8** Kwa maana urefu wa vyumba vya kulia chakula vilivyokuwa vikielekea ua wa nje ulikuwa mikono 50, na, tazama! mbele ya hekalu mikono 100. **9** Na kutoka upande wa chini wa vyumba hivyo vya kulia chakula njia ya kuingilia ilielekea mashariki, mtu anapoingia akitoka ua wa nje.

10 Katika upana wa ule ukuta wa mawe kuelekea mashariki, mbele ya lile eneo lililotengwa[b] na mbele ya jengo, kulikuwa na vyumba vya kulia chakula.[c] **11** Na kulikuwa na njia mbele yake inayofanana na vile vyumba vya kulia chakula vilivyokuwa vikielekea kaskazini,[d] hivyo ndivyo urefu wake ulivyokuwa na ndivyo upana wake ulivyokuwa; na milango yake yote ya kutokea ilifanana, nazo ramani zake zilifanana na miingilio yake ilifanana. **12** Na kama ilivyokuwa ile miingilio ya vyumba vya kulia chakula iliyoelekea kusini ndivyo ulivyokuwa ule mwingilio mbele ya njia, njia iliyo mbele ya ukuta unaolingana wa mawe kuelekea mashariki, mtu anapoiingia.[e]

SURA 42

a 1Fa 6:8
Eze 41:6

b Eze 41:12

c Eze 42:1

d Eze 42:4

e Eze 42:9

Safu ya 2

a Eze 42:1

b Hes 16:5
Kum 21:5
Eze 40:46

c Law 6:16
Law 7:6
Law 10:13
Law 24:9
Hes 18:10

d Law 2:3
Hes 18:9
Ne 13:5

e Kut 28:40
Kut 29:8
Law 8:13
Eze 44:19

f Isa 61:10

g Eze 40:6

h Eze 40:5

13 Naye akaniambia: "Vyumba vya kulia chakula vya kaskazini na vyumba vya kulia chakula vya kusini ambavyo viko mbele ya eneo lililotengwa,[a] hivyo ndivyo vyumba vya kulia chakula vilivyo vitakatifu, ambamo makuhani wanaomkaribia[b] Yehova hula vitu vitakatifu zaidi.[c] Humo wao huweka vitu vilivyo vitakatifu zaidi na toleo la nafaka na toleo la dhambi na toleo la hatia, kwa sababu mahali hapo ni patakatifu.[d] **14** Wakati hao, makuhani, wakiisha kuingia, wao pia hawatatoka nje kutoka katika mahali patakatifu mpaka kwenye ua wa nje, lakini humo watayaweka mavazi yao ambayo wao huyavaa kwa ukawaida wakihudumu,[e] kwa maana hayo ni kitu kitakatifu. Watavaa mavazi mengine,[f] nao watakikaribia kile kinachohusiana na watu."

15 Naye akamaliza vipimo vya nyumba ya ndani, naye akanitoa nje kupitia lango ambalo upande wake wa mbele ulielekea mashariki,[g] naye akalipima kuzunguka pande zote.

16 Akapima upande wa mashariki kwa ule utete wa kupimia. Ulikuwa tete mia tano, kwa utete wa kupimia,[h] kuzunguka pande zote.

17 Akapima upande wa kaskazini, tete mia tano, kwa utete wa kupimia, kuzunguka pande zote.

18 Upande wa kusini akaupima, tete mia tano, kwa utete wa kupimia.

19 Akazunguka upande wa magharibi. Akapima tete mia tano, kwa utete wa kupimia.

20 Akazipima zile pande nne.
Kulikuwa na ukuta kuzunguka pande zote,[a] wenye urefu
wa tete mia tano na upana wa
tete mia tano,[b] ili kutenganisha kilicho kitakatifu na kilicho
najisi.[c]

43 Kisha akanifanya niende kwenye lango, lango linaloelekea mashariki.[d] **2** Na, tazama! utukufu[e]
wa Mungu wa Israeli ulikuwa
ukija kutoka upande wa mashariki,[f] nayo sauti yake ilikuwa kama sauti ya maji mengi;[g] nayo dunia yenyewe ikang'aa kwa sababu ya utukufu wake.[h] **3** Nayo ilionekana
kama maono niliyokuwa nimeona,[i] kama maono niliyoona
nilipokuja kuliharibu jiji;[j] pia kulionekana vitu kama nilivyoona kando ya mto Kebari,[k] nami
nikaanguka kifudifudi.

4 Na utukufu[l] wa Yehova
ukaingia ndani ya Nyumba
kupitia lango ambalo upande
wake wa mbele ulielekea mashariki.[m] **5** Na roho ikaniinua[n] na kuniingiza ndani ya ua
wa ndani, na, tazama! Nyumba
hiyo ilikuwa imejaa utukufu
wa Yehova.[o] **6** Nami nikaanza kusikia mtu akisema nami
kutoka katika Nyumba[p] hiyo,
naye mtu huyo akaja kusimama kando yangu.[q] **7** Naye
akaniambia:

"Mwana wa binadamu, hapa
ndipo mahali pa kiti changu
cha ufalme[r] na mahali pa nyayo za miguu yangu,[s] ambapo
nitakaa katikati ya wana wa
Israeli mpaka wakati usio na
kipimo;[t] nao, nyumba ya Israeli, hawataendelea tena kulitia unajisi jina langu takatifu,[a] wao na wafalme wao,[b] kwa
uasherati wao na kwa mizoga[c] ya wafalme wao wakati
wanapokufa, **8** kwa kuweka kwao kizingiti chao pamoja na kizingiti changu na mwimo wa mlango wao kando ya
mwimo wa mlango wangu, kukiwa na ukuta kati yangu na
wao.[d] Nao walilitia unajisi jina
langu takatifu kwa machukizo yao ambayo walifanya,[e] hivi
kwamba nikawaangamiza katika hasira yangu.[f] **9** Sasa na
wauondolee mbali nami uasherati[g] wao na mizoga ya wafalme wao,[h] nami hakika nitakaa
katikati yao mpaka wakati usio
na kipimo.[i]

10 "Na wewe, Ee mwana wa
binadamu, iambie nyumba ya
Israeli kuhusu ile Nyumba,[j] ili
wafedheheke kwa sababu ya
makosa yao,[k] nao lazima wapime kielelezo hicho. **11** Na
ikiwa kwa kweli watafedheheka kwa sababu ya mambo yote
ambayo wamefanya, ramani
ya ile Nyumba,[l] na mpangilio wake na njia zake za kutokea na za kuingilia, na ramani zake zote na vipimo vyake vyote, na ramani zake zote
na sheria zake zote uwajulishe na kuziandika machoni
pao, ili wapate kuona ramani
zake zote na vipimo vyake vyote nao kwa kweli wafanye hivyo.[m] **12** Hii ndiyo sheria ya
Nyumba hiyo. Juu ya mlima
eneo lake lote kuzunguka pande zote ni kitu kitakatifu zaidi.[n] Tazama! Hii ndiyo sheria ya
Nyumba hiyo.

13 "Na hivi ndivyo vipimo
vya madhabahu kwa kipimo
cha mikono,[o] mkono mmoja
ukiwa ni mkono mmoja na upa-

SURA 42

a Eze 40:5
b Eze 45:2
c Law 10:10
Eze 22:26
Eze 44:23
2Ko 6:17
Ufu 21:27

SURA 43

d Eze 10:19
Eze 40:6
Eze 42:15
Eze 44:1
e Isa 6:3
Eze 3:23
Eze 9:3
f Eze 11:23
g Zb 29:3
Eze 1:24
Yoh 12:29
h Isa 60:1
Eze 10:4
Hab 2:14
Ufu 21:23
i Eze 1:4
j Yer 1:10
k Eze 1:3
Eze 3:23
l Eze 10:19
m Eze 44:2
n Eze 3:12
Eze 8:3
Eze 11:24
o Kut 40:34
1Fa 8:10
2Nya 5:14
Isa 6:3
Eze 44:4
p Ufu 16:1
q Eze 40:3
r Zb 47:8
Isa 6:1
Yer 3:17
Eze 1:26
s 1Nya 28:2
Zb 99:5
t Kut 29:45
Zb 68:16
Zb 132:14
Yoe 3:17
2Ko 6:16

Safu ya 2

a Eze 39:7
Ho 14:8
Zek 13:2
b 1Fa 11:7
2Fa 21:2
2Nya 33:7
c Yer 16:18
d 2Fa 16:14
Eze 8:3
e Amo 2:7
f Da 9:12
g Ho 2:2
h Eze 37:23
i Eze 37:26
2Ko 6:16
j Eze 40:4
k Eze 16:63
Ro 6:21
l Eze 44:5
Ebr 8:5
m Eze 11:20
Eze 36:27
Yoh 13:17
n Zb 93:5
Eze 40:2
Eze 42:20
o Kut 27:1
2Nya 4:1

na wa kiganja[a] kimoja. Nayo se-
hemu yake ya chini ni mkono
mmoja. Na mkono mmoja upa-
na wake. Na mpaka wake uko
juu ya mdomo wake kuzunguka pande zote, shubiri moja.
Na huo ndio msingi wa madha-
bahu. **14** Na kutoka sehemu
ya chini kwenye sakafu mpa-
ka kwenye rafu ya chini ina-
yozunguka kuna mikono miwi-
li, nao upana ni mkono mmo-
ja. Na kutoka ile rafu ndogo
mpaka kwenye ile rafu ku-
bwa inayozunguka kuna miko-
no minne, nao upana wake ni
mkono mmoja. **15** Nayo ma-
jiko ya madhabahu ni miko-
no minne, na kutoka kwenye
majiko ya madhabahu kuele-
kea juu kuna zile pembe nne.[b]
16 Nayo majiko ya madhaba-
hu yana urefu wa mikono kumi
na miwili, na upana wa miko-
no kumi na miwili,[c] mraba pa-
nde zake nne.[d] **17** Nayo rafu
inayozunguka ina urefu wa mi-
kono kumi na minne, na upa-
na wa mikono kumi na minne,
pande zake nne; nao mpaka
unaozunguka ni nusu mkono,
nayo sehemu yake ya chini ni
mkono mmoja kuzunguka pa-
nde zote.

"Nazo ngazi zake zinaelekea
mashariki."

18 Naye akaniambia: "Mwa-
na wa binadamu, Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova amese-
ma hivi, 'Hizi ndizo sheria za
madhabahu katika siku ile ya
kuifanya, ili kutoa juu yake
matoleo mazima ya kuketete-
zwa[e] na kunyunyiza damu juu
yake.'[f]

19 "'Nawe utawapa makuha-
ni Walawi,[g] ambao ni uzao wa
Sadoki,[h] wale wanaonikaribia
mimi,'[a] asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova, 'ili kunihudu-
mia, ng'ombe-dume mchanga,
mwana wa mifugo, awe toleo
la dhambi.[b] **20** Nawe utachu-
kua sehemu ya damu yake na
kuitia kwenye zile pembe zake
nne na juu ya ncha nne za rafu
inayozunguka na juu ya mpa-
ka unaozunguka pande zote na
kuitakasa kutokana na dhambi[c]
na kufanya upatanisho kwa aji-
li yake.[d] **21** Nawe utamchu-
kua yule ng'ombe-dume mcha-
nga, lile toleo la dhambi, na la-
zima mtu aliteketeze katika
mahali palipochaguliwa pa ile
Nyumba, nje ya patakatifu.[e]
22 Na siku ya pili utaleta ka-
ribu dume la mbuzi, ambaye
hana kasoro, awe toleo la dha-
mbi; nao wataitakasa madha-
bahu kutokana na dhambi
kama vile walivyoitakasa
kutokana na dhambi kwa yule
ng'ombe-dume mchanga.'

23 "'Wakati utakapomaliza
kutakasa kutokana na dha-
mbi utamleta karibu ng'ombe-
dume mchanga, mwana wa mi-
fugo, ambaye hana kasoro,
na kondoo-dume kutoka kati-
ka kundi, ambaye hana kaso-
ro. **24** Nawe utawaleta kari-
bu mbele za Yehova, nao ma-
kuhani watatupa chumvi juu
yao na kuwatoa[f] kwa Yehova
wakiwa toleo zima la kuketete-
zwa. **25** Kwa siku saba uta-
mtoa mbuzi-dume akiwa toleo
la dhambi kila siku;[g] na ng'o-
mbe-dume mchanga, mwana
wa mifugo, na kondoo-dume
kutoka katika kundi, ambao
hawana kasoro, watawatoa.
26 Kwa siku saba watafanya
upatanisho[h] kwa ajili ya ma-
dhabahu, nao wataitakasa na

SURA 43

a Eze 40:5

b Kut 27:2
Ufu 9:13

c 2Nya 4:1

d Kut 38:1

e Kut 40:29

f Law 1:5
Law 8:19
Eze 45:19

g Isa 61:6
Yer 33:18
1Pe 2:5

h Eze 40:46
Eze 44:15
Eze 48:11

Safu ya 2

a Hes 16:40

b Kut 29:10
Law 8:14
Ebr 7:27

c Kut 29:36
Law 4:26

d Law 8:15
Law 16:19
Ebr 9:23

e Kut 29:14
Law 8:17
Ebr 13:11

f Law 2:13

g Kut 29:35

h Law 8:34

kuiweka rasmi. **27** Nao watamaliza siku hizo. Na itakuwa kwamba katika siku ya nane[a] na kuanzia hapo na kuendelea makuhani watatoa juu ya madhabahu matoleo yenu mazima ya kuteketezwa na dhabihu zenu za ushirika; nami hakika nitapendezwa nanyi,'[b] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova."

44 Naye akanirudisha kupitia lango la patakatifu, lile la nje linaloelekea mashariki,[c] nalo lilikuwa limefungwa.[d] **2** Ndipo Yehova akaniambia: "Lango hili, litakaa likiwa limefungwa. Halitafunguliwa, na hakuna mtu wa vivi hivi tu atakayeliingilia; kwa maana Yehova mwenyewe, Mungu wa Israeli,[e] ameliingilia, nalo litakaa likiwa limefungwa. **3** Hata hivyo, mkuu[f]—kwa kuwa yeye ni mkuu ataketi humo, ili ale mkate mbele za Yehova.[g] Ataingia kupitia ukumbi wa lango, na kupitia hapo atatoka."[h]

4 Naye sasa akanileta kupitia lango la kaskazini mpaka mbele ya ile Nyumba, nipate kuona, na, tazama! utukufu wa Yehova ulikuwa umeijaza nyumba ya Yehova.[i] Nami nikaanguka kifudifudi.[j] **5** Ndipo Yehova akaniambia: "Mwana wa binadamu, weka moyoni mwako[k] na uone kwa macho yako, na kwa masikio yako usikie yote ninayokuambia kuhusu kanuni zote za nyumba ya Yehova na kuhusu sheria zake zote, nawe utauweka moyo wako juu ya njia ya kuingilia ya ile Nyumba pamoja na mahali pote pa kutokea pa patakatifu. **6** Nawe utamwambia Uasi,[a] nyumba ya Israeli, 'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Inatosha, kwa sababu ya machukizo yenu yote, Ee nyumba ya Israeli,[b] **7** mnapowaingiza ndani wageni ambao hawajatahiriwa moyoni na ambao hawajatahiriwa katika mwili,[c] ili wawe ndani ya patakatifu pangu na kupatia unajisi, naam, nyumba yangu; mnapotoa mkate[d] wangu, mafuta[e] na damu,[f] huku wakiendelea kuvunja agano langu kwa sababu ya machukizo yenu yote.[g] **8** Wala hamjautunza wajibu wa vitu vyangu vitakatifu,[h] wala hamkuwaweka wengine kwa ajili yenu wawe watunzaji wa wajibu wangu katika patakatifu pangu."'[i]

9 "'Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Hakuna mgeni yeyote, ambaye hajatahiriwa moyoni na ambaye hajatahiriwa katika mwili, atakayeingia ndani ya patakatifu pangu, yaani, mgeni yeyote aliye katikati ya wana wa Israeli."'[j]

10 "'Lakini Walawi walioenda mbali nami[k] wakati ambapo Israeli, aliyeondoka akaenda mbali nami, alienda kufuatilia sanamu zao za mavi, wao pia lazima wachukue kosa lao.[l] **11** Na katika patakatifu pangu watakuwa wahudumu katika vyeo vya uangalizi juu ya malango ya ile Nyumba na wahudumu kwenye ile Nyumba.[m] Wao wenyewe watachinja toleo zima la kuteketezwa na dhabihu kwa ajili ya watu,[n] na wao wenyewe watasimama

SURA 43
a Law 9:1
b Ayu 42:8
Eze 20:40
Ro 12:1
1Pe 2:5

SURA 44
c Eze 43:1
d Eze 46:1
e Kut 24:10
Eze 43:2
f Zb 45:16
Isa 32:1
g Mwa 31:54
Kum 12:7
1Ko 10:18
h Eze 40:9
Eze 46:2
i Isa 6:3
Eze 3:23
Eze 10:4
j Mwa 17:3
Eze 1:28
k Kum 32:46
2Nya 11:16
Met 24:32
Eze 40:4

Safu ya 2
a Kum 31:27
Isa 1:20
Isa 30:9
Eze 2:5
b Eze 45:9
1Pe 4:3
c Law 22:25
Mdo 21:28
d Law 21:6
Mal 1:7
e Law 3:16
f Law 17:11
g Law 26:15
Kum 31:16
Yer 11:10
Ebr 8:9
h Law 22:2
Hes 18:3
Mdo 7:53
i 1Nya 23:32
j Zb 50:16
Yoe 3:17
Zek 14:21
k 2Fa 23:8
2Nya 29:5
Ne 9:34
Yer 23:11
Eze 8:12
l Eze 48:11
m 1Nya 26:1
n 2Nya 29:34

mbele yao ili kuwahudumia.[a]
12 Kwa sababu waliendelea
kuwahudumia mbele ya sana-
mu zao za mavi[b] na kuwa ki-
kwazo cha kuingiza ndani ya
dhambi kwa nyumba ya Israe-
li,[c] ndiyo sababu nimeuinua
mkono wangu juu yao,'[d] asema
Bwana Mwenye Enzi Kuu Ye-
hova, 'nao watalichukua kosa
lao. **13** Nao hawatanikaribia
ili kutenda kama kuhani kwa-
ngu au kukaribia chochote
kati ya vitu vyangu vilivyo vi-
takatifu,[e] vilivyo vitakatifu za-
idi, nao watachukua fedheha
yao na machukizo yao waliyo-
yafanya.[f] **14** Nami hakika ni-
tawafanya wao kuwa watunza-
ji wa wajibu wa ile Nyumba, ku-
husu utumishi wake wote na
kuhusu yote ambayo yanapasa
kufanywa ndani yake.'[g]

15 "'Nao makuhani Wala-
wi,[h] wana wa Sadoki,[i] ambao
walitunza wajibu wa patakati-
fu pangu wakati ambapo wana
wa Israeli waliondoka waka-
enda mbali nami,[j] wao wenye-
we watanikaribia na kunihudu-
mia, nao watasimama mbele zan-
gu[k] na kunitolea mafuta[l] na
damu,'[m] asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova. **16** 'Hao
ndio watakaoingia katika pata-
katifu pangu,[n] na wao wenyewe
wataikaribia meza yangu ili ku-
nihudumia,[o] nao watauangalia
wajibu wangu.[p]

17 "'Na itatukia kwamba
watakapoingia ndani ya mala-
ngo ya ua wa ndani, wanapa-
swa kuvaa mavazi ya kitani,
na wasivae sufu yoyote wana-
pohudumu katika malango ya
ua wa ndani na wakiwa ndani.[q]
18 Vitambaa vya kichwa vya

SURA 44
a Hes 16:9
b Eze 6:13
c Isa 9:16
Mal 2:8
d Kum 32:40
Zb 106:26
e Hes 18:3
2Fa 23:9
f Eze 32:30
g Hes 18:4
1Nya 23:28
1Nya 23:32
h Eze 40:46
Eze 43:19
i 1Fa 2:35
j Eze 44:10
Eze 48:11
k Kum 10:8
Eze 43:19
l Law 3:16
m Law 17:6
n Ufu 1:6
o Eze 41:22
Mal 1:7
p Hes 18:7
q Kut 28:39
Kut 39:27
Law 16:4
Ufu 19:8

Safu ya 2
a Kut 28:40
Kut 39:28
b Kut 28:42
c Law 6:10
Eze 42:14
d Eze 42:13
e Kut 30:29
Law 6:27
f Law 21:5
Kum 14:1
g 1Ko 11:14
h Law 10:9
Lu 1:15
i Law 21:7
j Law 21:14
k Law 10:10
Eze 22:26
Mal 2:7
l Kum 17:9
m 1Nya 23:4
2Nya 19:8
n Law 23:2
o Isa 58:13
Eze 22:26

kitani ndivyo vitakavyokuwa
kichwani pao,[a] na suruali za ki-
tani ndizo zitakazokuwa viu-
noni mwao.[b] Wasijifunge cho-
chote ambacho husababisha
jasho. **19** Na wanapoenda
kwenye ua wa nje, hata kwe-
nye ua wa nje kwa watu, wana-
paswa kuyavua mavazi yao wa-
liyokuwa wameyavaa wakihu-
dumu,[c] nao watayaweka kwe-
nye vyumba vitakatifu vya
kulia chakula[d] na kuvaa mava-
zi mengine, ili wasije wakawa-
takasa watu kwa mavazi yao.[e]
20 Nao hawapaswi kuvinyoa
vichwa vyao,[f] na nywele za
kichwa hawapaswi kuziacha
ziwe ndefu. Kwa vyovyote vile
wanapaswa wazikate nywele
za kichwa chao.[g] **21** Wala
makuhani wowote wasinywe
divai yoyote wanapoingia nda-
ni ya ua wa ndani.[h] **22** Nao
hawatamwoa mjane au mwa-
namke yeyote aliyetalikiwa,[i]
lakini wanaweza kuoa mabikira
wa uzao wa nyumba ya Israe-
li[j] au mjane ambaye ni mjane
wa kuhani.'

23 "'Nao watawafundisha
watu wangu tofauti kati ya
kitu kitakatifu na kitu najisi;
nao watawajulisha watu tofau-
ti kati ya kitu ambacho si safi
na kitu safi.[k] **24** Na katika
kesi wao wenyewe watasima-
ma ili kuhukumu;[l] wataihuku-
mu pia kwa maamuzi yangu ya
hukumu.[m] Nazo sheria zangu
na kanuni zangu kuhusiana na
majira yangu yote ya sherehe[n]
watazishika, nazo sabato za-
ngu watazitakasa.[o] **25** Wala
asiingie kwa mtu aliyekufa
ajitie uchafu, lakini kwa aji-
li ya baba au mama au mwa-
na au binti au ndugu au dada

ambaye hajaolewa wanaweza kujitia uchafu.[a] **26** Na baada ya yeye kutakaswa, wanapaswa kumhesabia siku saba.[b] **27** Na katika siku atakayoingia ndani ya patakatifu, ndani ya ua wa ndani, ili kuhudumu ndani ya patakatifu, anapaswa kutoa toleo lake la dhambi,'[c] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

28 "'Nao utakuwa urithi wao: Mimi ndiye urithi wao.[d] Nanyi msiwape mali yoyote katika Israeli: Mimi ndiye mali yao. **29** Toleo la nafaka na toleo la dhambi na toleo la hatia—hao ndio watakaokula hayo.[e] Na kila kitu kilichotolewa katika Israeli—kitakuwa chao.[f] **30** Na ya kwanza kati ya matunda ya kwanza yaliyoiva ya kila kitu na kila mchango wa kila kitu kutoka katika michango yenu yote—yatakuwa ni ya makuhani;[g] na matunda ya kwanza ya unga wenu wenye chenga-chenga mtawapa makuhani,[h] ili kufanya baraka ikae juu ya nyumba yako.[i] **31** Makuhani wasile mnyama yeyote aliyekufa tayari wala kiumbe chochote kilichoraruliwa vipande-vipande kati ya viumbe vinavyoruka au kati ya wanyama.'[j]

45 "'Na wakati ninyi mtakapoigawa nchi iwe urithi,[k] mtamtolea Yehova mchango,[l] fungu takatifu kutoka katika nchi;[m] urefu wake utakuwa mikono 25,000, nao upana wake 10,000.[n] Litakuwa fungu takatifu katika mipaka yake yote kuzunguka pande zote. **2** Kutoka katika hilo kutakuwako kwa ajili ya mahali patakatifu fungu la urefu wa 500 kwa upana wa 500, likiwa mraba kuzunguka pande zote;[a] nalo litakuwa na kiwanja cha malisho cha mikono 50 kila upande.[b] **3** Na kutoka katika kipimo hicho utapima urefu wa 25,000 na upana wa 10,000, na patakatifu patakuwa ndani yake, kitu kitakatifu zaidi.[c] **4** Litakuwa fungu takatifu kutoka katika nchi kwa ajili ya makuhani wenyewe,[d] wahudumu wa patakatifu, wale wanaokaribia ili kumhudumia Yehova.[e] Na hapo patakuwa mahali pa nyumba kwa ajili yao, na mahali patakatifu kwa ajili ya patakatifu.

5 "'Urefu utakuwa 25,000 nao upana wake utakuwa 10,000.[f] Patakuwa pa Walawi, wahudumu wa ile Nyumba. Nao watamiliki vyumba 20 vya kulia chakula.[g]

6 "'Na miliki ya jiji, mtatoa upana wa 5,000 na urefu wa 25,000, sawasawa na mchango mtakatifu.[h] Itakuwa ya nyumba yote ya Israeli.

7 "'Na kwa ajili ya mkuu kutakuwako upande huu na upande ule wa mchango mtakatifu na wa miliki ya jiji, mbali na ule mchango mtakatifu[i] na ile miliki ya jiji, kitu fulani upande wa magharibi kuelekea magharibi na kitu upande wa mashariki kuelekea mashariki. Nao urefu utakuwa sawasawa na moja kati ya yale mafungu, kutoka mpaka wa magharibi hadi mpaka wa mashariki.[j] **8** Nayo nchi, itakuwa mali yake katika Israeli. Nao wakuu wangu hawataendelea kuwatendea vibaya

SURA 44
a Law 21:2
b Hes 19:12
c Law 4:3
Law 8:14
d Hes 18:20
Kum 10:9
Kum 18:1
Yos 13:14
Yos 13:33
Eze 45:4
e Law 2:3
Law 6:18
Law 7:6
1Ko 9:13
Ebr 13:10
f Law 27:21
Hes 18:14
g Kut 23:19
Hes 3:13
Hes 18:12
Hes 18:27
Kum 18:4
2Nya 31:4
2Nya 31:10
Ne 10:35
h Hes 15:20
Ne 10:37
i Met 3:9
Mal 3:10
j Kut 22:31
Law 22:8
Kum 14:21

SURA 45
k Yos 14:2
Eze 47:22
l Met 3:9
Eze 48:8
m Eze 48:20
n Eze 48:9

Safu ya 2
a Eze 42:20
b Yos 21:2
c Eze 48:10
d Eze 48:11
e Hes 16:5
Eze 40:46
Eze 43:19
f Eze 48:10
Eze 48:13
g 1Nya 9:26
Eze 40:17
h Eze 48:15
i Eze 46:16
j Eze 48:21

tena watu wangu,[a] nao wataipa nyumba ya Israeli nchi hiyo
kulingana na makabila yao.'[b]
9 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi,
'Imetosha, enyi wakuu wa
Israeli!'[c]
"'Ondoeni jeuri na uporaji,[d]
na mfanye haki na uadilifu.[e]
Acheni kutumia uwezo vibaya
kuchukua vitu vya watu wa-
ngu,'[f] asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova. **10** 'Mna-
paswa kuwa na mizani sahihi
na efa sahihi na kipimo sahihi
cha bathi.[g] **11** Na kuhusu efa
na kipimo cha bathi, kutakuwa
na kiwango kimoja kamili, ili
kipimo cha bathi kichukue se-
hemu ya kumi ya homeri na se-
hemu ya kumi ya homeri ichu-
kue efa;[h] kuhusiana na home-
ri, kiwango chake kinachohi-
tajiwa kinapaswa kuwa hicho.
12 Nayo shekeli[i] ni gera 20.[j]
Shekeli 20, shekeli 25, sheke-
li 15 ndizo zitakazokuwa mane
moja kwako.'
13 "'Huu ndio mchango
ambao utautoa, sehemu ya sita
ya efa kutoka katika homeri
ya ngano, na sehemu ya sita
ya efa kutoka katika home-
ri ya shayiri; **14** na kuhusu
posho la mafuta, kuna kipimo
cha bathi cha mafuta. Bathi ni
sehemu ya kumi ya kori. Ba-
thi kumi ni homeri moja; kwa
sababu bathi kumi ni home-
ri moja. **15** Na kondoo mmo-
ja kutoka katika kundi, kuto-
ka katika mifugo mia mbili ya
Israeli,[k] kwa ajili ya toleo la
nafaka[l] na kwa ajili ya toleo
zima la kuteketezwa[m] na kwa
ajili ya dhabihu za ushirika,[n]
ili kufanya upatanisho kwa aji-
li yao,'[a] asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova.
16 "'Nao watu wote wa nchi,
watakuwa na wajibu wa kutoa
mchango[b] huu kwa mkuu ka-
tika Israeli.[c] **17** Naye mkuu[d]
atakuwa na wajibu juu ya ma-
toleo mazima ya kuteketezwa[e]
na toleo la nafaka[f] na toleo
la kinywaji[g] wakati wa she-
rehe[h] na wakati wa miezi mi-
pya[i] na wakati wa sabato,[j] wa-
kati wa majira yote ya shere-
he ya nyumba ya Israeli.[k] Yeye
ndiye atakayetoa toleo la dha-
mbi na toleo la nafaka na toleo
zima la kuteketezwa na dhabi-
hu za ushirika, ili kufanya upa-
tanisho kwa ajili ya nyumba ya
Israeli.'
18 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema hivi,
'Katika mwezi wa kwanza,
siku ya kwanza ya mwezi huo,
utamchukua ng'ombe-dume
mchanga, mwana wa mifugo,
ambaye hana kasoro,[l] nawe
utapatakasa patakatifu kuto-
kana na dhambi.[m] **19** Naye
kuhani atachukua sehemu ya
damu ya toleo la dhambi na ku-
iweka kwenye mwimo wa mla-
ngo[n] wa ile Nyumba na juu ya
zile pembe nne za rafu ya ma-
dhabahu[o] inayozunguka na juu
ya mwimo wa lango la ua wa
ndani. **20** Na hivyo ndivyo
utakavyofanya katika siku ya
saba ya mwezi kwa sababu ya
mtu yeyote anayefanya kosa[p]
na kwa sababu ya mtu yeyo-
te ambaye hana uzoefu; nanyi
mtafanya upatanisho kwa ajili
ya ile Nyumba.[q]
21 "'Katika mwezi wa kwa-
nza, siku ya kumi na nne ya
mwezi huo, mtafanya pasaka.[r]
Hiyo ikiwa ni sherehe ya siku

SURA 45
a Met 28:16
Isa 32:1
Isa 60:17
Yer 22:17
Yer 23:5
Eze 22:27
Eze 46:18
Mik 3:1
b Yos 11:23
c Eze 44:6
d Ne 5:10
Zb 82:2
Isa 1:17
e Yer 22:3
Mik 6:8
Zek 8:16
f Ayu 24:2
Mik 2:2
g Law 19:36
Met 11:1
Met 16:11
Met 20:10
Amo 8:5
Mik 6:11
h Kut 16:36
i Kut 30:13
Law 27:25
j Hes 3:47
k Met 3:9
l Law 2:1
m Law 1:10
n Law 3:1

Safu ya 2
a Law 1:4
Law 6:30
Ebr 9:22
b Kut 30:14
c Isa 16:1
d Eze 45:22
e 1Nya 16:2
2Nya 30:24
f 1Fa 8:64
g Ezr 6:9
h 2Nya 35:7
i 2Nya 8:13
2Nya 31:3
j Isa 66:23
k Law 23:2
l Law 22:20
m Law 16:16
Eze 43:26
n Eze 41:21
Eze 46:2
o Eze 43:20
p Law 4:27
Zb 19:12
q Law 16:20
r Law 23:5
Hes 9:2
Hes 28:16
Kum 16:1

saba, keki zisizo na chachu
ndizo zitakazoliwa.[a] **22** Na
katika siku hiyo, kwa ajili
yake mwenyewe na kwa ajili
ya watu wote wa nchi, mkuu
atatoa ng'ombe-dume mcha-
nga kuwa toleo la dhambi.[b]
23 Na kwa siku hizo saba za
sherehe[c] atamtolea Yehova to-
leo zima la kuteketezwa la ng'o-
mbe-dume saba wachanga na
kondoo-dume saba, ambao ha-
wana kasoro, kila siku kwa siku
saba,[d] na kuwa toleo la dha-
mbi atatoa dume la mbuzi kila
siku.[e] **24** Naye atatoa toleo la
nafaka la efa kwa ajili ya yule
ng'ombe-dume mchanga na efa
kwa ajili ya yule kondoo-dume,
na, kwa habari ya mafuta, hini
moja kwa efa.[f]

25 "'Katika mwezi wa saba,
katika siku ya kumi na tano
ya mwezi huo, wakati wa she-
rehe,[g] atatoa vitu vivyo hivyo
kwa siku saba,[h] vivyo hivyo
kwa habari ya toleo la dhambi,
toleo zima la kuteketezwa, na
toleo la nafaka na mafuta.'"

46 "Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova amesema
hivi, 'Kwa habari ya lango la
ua wa ndani linaloelekea ma-
shariki,[i] litakaa likiwa limefu-
ngwa[j] kwa siku sita za kazi,[k]
na katika siku ya sabato lita-
funguliwa, na katika siku ya
mwezi mpya litafunguliwa.[l]
2 Naye mkuu ataingia kupi-
tia kwenye ukumbi wa lango,[m]
kutoka nje, na kusimama ka-
ndo ya mwimo wa lango;[n] nao
makuhani watatoa toleo lake
zima la kuteketezwa na dhabi-
hu zake za ushirika, naye ata-
inama penye kizingiti cha la-
ngo,[o] naye atatoka nje, laki-
ni lango lenyewe halitafungwa
mpaka jioni. **3** Nao watu wa
nchi watainama kwenye kizi-
ngiti cha lango hilo katika siku
za sabato na katika miezi mi-
pya, mbele za Yehova.[a]

4 "'Nalo toleo zima la kute-
ketezwa ambalo mkuu atamto-
lea Yehova katika siku ya saba-
to litakuwa wana-kondoo sita
ambao hawana kasoro na ko-
ndoo-dume mmoja ambaye
hana kasoro;[b] **5** na toleo la
nafaka la efa moja kwa ajili ya
yule kondoo-dume,[c] na kwa aji-
li ya wale wana-kondoo toleo
la nafaka kulingana na uwezo
wake wa kutoa,[d] na, kwa ha-
bari ya mafuta, hini moja
kwa efa.[e] **6** Na siku ya mwe-
zi mpya[f] kutakuwa na ng'o-
mbe-dume mchanga, mwana
wa mifugo, ambaye hana kaso-
ro, na wana-kondoo sita na ko-
ndoo-dume mmoja; hawapaswi
kuwa na kasoro.[g] **7** Naye ata-
toa toleo la nafaka la efa moja
kwa ajili ya yule ng'ombe-
dume mchanga na efa moja
kwa ajili ya yule kondoo-dume,
na kwa ajili ya wale wana-ko-
ndoo atatoa kulingana na uwe-
zo wake; na, kwa habari ya ma-
futa, hini moja kwa efa.[h]

8 "'Naye mkuu[i] anapoingia
ndani, ataingia kupitia njia
ya ukumbi wa lango, naye ata-
toka nje kupitia njia hiyo.[j]
9 Na watu wa nchi hiyo wana-
poingia ndani mbele za Yeho-
va katika majira ya sherehe,[k]
yeye anayeingia kupitia njia ya
lango la kaskazini[l] ili kuinama
atatoka nje kupitia njia ya la-
ngo la kusini;[m] na yule anayei-
ngia kupitia njia ya lango la ku-
sini atatoka nje kupitia njia ya

SURA 45
a Kut 12:18
Law 23:6
b Law 4:14
c Law 23:8
d Ayu 42:8
e Hes 28:15
f Eze 46:5
g Law 23:34
2Nya 5:3
h Hes 29:12
Kum 16:13
2Nya 7:8
Zek 14:16

SURA 46
i Eze 40:32
j Eze 44:2
k Kut 20:9
l Zb 81:3
Isa 66:23
m Eze 44:3
n Eze 41:21
o 2Nya 29:29

Safu ya 2
a Isa 66:23
Lu 1:10
b Hes 28:9
Eze 45:17
c Hes 28:12
Eze 45:24
d Kum 16:17
e Law 14:21
Eze 46:11
f Amo 8:5
g 1Nya 23:31
h Kut 16:36
Eze 45:24
i Eze 45:16
Eze 45:22
j Eze 46:2
k Kut 23:14
Kum 16:16
l Eze 40:20
m Eze 40:24

lango la kaskazini. Mtu yeyote asirudi kupitia njia ya lango aliloingilia, kwa maana anapaswa kutoka nje moja kwa moja mbele yake. **10** Na kwa habari ya mkuu aliye katikati yao, wakati wao wanapoingia ndani, yeye ataingia ndani; na wakati wao wanapotoka nje, yeye atatoka nje.[a] **11** Na katika sherehe[b] na katika majira ya sherehe toleo la nafaka litakuwa efa moja kwa ajili ya yule ng'ombe-dume mchanga na efa moja kwa ajili ya yule kondoo-dume, na kwa ajili ya wale wana-kondoo kulingana na uwezo wake wa kutoa; na, kwa habari ya mafuta, hini moja kwa efa.[c]

12 "'Na ikiwa mkuu atatoa toleo la hiari ili liwe toleo zima la kuteketezwa,[d] au dhabihu za ushirika ziwe toleo la hiari kwa Yehova, mtu atamfungulia pia lango linaloelekea mashariki,[e] naye atatoa toleo lake zima la kuteketezwa na dhabihu zake za ushirika kama vile anavyofanya siku ya sabato.[f] Naye atatoka nje, na mtu atalifunga lango baada ya yeye kutoka nje.[g]

13 "'Na mwana-kondoo dume ambaye hana kasoro, aliye katika mwaka wake wa kwanza, utamtoa awe toleo zima la kuteketezwa kila siku kwa Yehova.[h] Utamtoa asubuhi baada ya asubuhi. **14** Na utatoa toleo la nafaka pamoja naye asubuhi baada ya asubuhi sehemu ya sita ya efa na, kwa habari ya mafuta, sehemu ya tatu ya hini ya kuunyunyizia unga laini.[i] Toleo la nafaka kwa Yehova ni sheria ya kudumu mpaka wakati usio na kipimo, daima. **15** Nao wataandaa mwana-kondoo dume na toleo la nafaka na mafuta asubuhi baada ya asubuhi kuwa toleo zima la kuteketezwa la daima.'

16 "Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Mkuu akimpa zawadi kila mmoja wa wanawe iwe urithi wake, huo wenyewe utakuwa mali ya wanawe wenyewe. Hiyo ndiyo miliki yao kulingana na urithi wao. **17** Na akimpa mmoja wa watumishi wake zawadi kutoka katika urithi wake, huo pia utakuwa wake mpaka ule mwaka wa uhuru;[a] nao utarudi kwa mkuu. Ni urithi wake tu—kwa habari ya wanawe—ndio utakaoendelea kuwa wao wenyewe. **18** Naye mkuu hatachukua urithi wowote wa watu ili kuwalazimisha waondoke katika miliki yao.[b] Atawapa wanawe urithi kutoka kwenye miliki yake mwenyewe, ili watu wangu wasitawanyike kila mmoja mbali na miliki yake.'"[c]

19 Naye akaniingiza ndani kupitia njia ya kuingilia[d] iliyokuwa kando ya lango mpaka kwenye vyumba vitakatifu vya kulia chakula, vile vya makuhani, vilivyoelekea kaskazini,[e] na, tazama! hapo palikuwa na mahali, pande zote mbili za nyuma kuelekea magharibi. **20** Naye akaniambia: "Hapa ndipo mahali ambapo makuhani watatokosea toleo la hatia[f] na toleo la dhambi,[g] na ambapo wataokea toleo la nafaka,[h] ili wasitoe chochote na kukipeleka kwenye ua wa nje ili kuwatakasa watu."[i]

SURA 46

a 2Nya 7:4

b Law 23:2 Hes 29:1 Kum 16:10

c Eze 45:24 Eze 46:7

d Law 1:3 1Fa 3:4

e Eze 46:1

f Eze 45:17

g Eze 46:2

h Kut 29:38 Hes 28:3

i Hes 28:5

Safu ya 2

a Law 25:10

b 1Fa 21:19 Eze 22:27

c Eze 34:5

d Eze 42:9

e Eze 42:1

f Kut 29:31 2Nya 35:13

g Eze 44:29

h Law 2:4 Law 2:5

i Eze 44:19

21 Naye akanitoa nje mpaka kwenye ua wa nje na kunipitisha kwenye ile miimo minne ya pembeni ya ule ua, na, tazama! kulikuwa na ua karibu na mwimo huu wa pembeni wa ule ua, ua ulio karibu na mwimo ule wa pembeni wa ua. **22** Katika ile miimo minne ya ua kulikuwa na nyua ndogo, zenye urefu wa mikono 40 na mikono 30 upana wake. Zote nne zikiwa zina miundo ya pembeni zilikuwa na kipimo kilekile. **23** Na kulikuwa na mstari kuzizunguka pande zote, kuzizunguka zote nne pande zote, na kulikuwa na mahali pa kutokosea[a] palipofanywa chini ya mistari hiyo kuzunguka pande zote. **24** Kisha akaniambia: "Hizi ni nyumba za wale wanaotokosa ambapo wahudumu wa ile Nyumba hutokosea dhabihu ya watu."[b]

47 Naye akanirudisha hatua kwa hatua mpaka kwenye mlango wa ile Nyumba,[c] na, tazama! kulikuwa na maji[d] yaliyokuwa yakitoka chini ya kizingiti cha Nyumba hiyo upande wa mashariki,[e] kwa maana upande wa mbele wa Nyumba ulikuwa mashariki. Nayo maji hayo yalikuwa yakishuka kutoka chini, kutoka upande wa kuume wa Nyumba hiyo, upande wa kusini wa madhabahu.

2 Naye akanileta hatua kwa hatua kupitia lango la kaskazini[f] na kunizungusha kupitia njia ya nje kwenda kwenye lango la nje linaloelekea mashariki,[g] na, tazama! maji[h] yalikuwa yanatiririka kutoka upande wa mkono wa kuume.

SURA 46
a 1Sa 2:13
b 2Nya 35:13 Eze 46:20

SURA 47
c Eze 41:2
d Yer 2:13 Zek 13:1 Zek 14:8
e Eze 43:4 Ufu 22:1
f Eze 40:20
g Eze 40:6 Eze 44:2
h Ufu 22:1

Safu ya 2
a Eze 40:3 Ufu 21:15
b Ufu 22:2
c Kum 4:49
d Yos 3:16
e Eze 47:18 Zek 14:8
f Mwa 1:20

3 Mtu huyo alipotoka kwenda mashariki akiwa na kamba ya kupimia mkononi mwake,[a] alipima pia mikono elfu moja na kunipitisha katikati ya maji yale, maji yanayofika kwenye vifundo vya miguu.

4 Naye akaendelea kupima elfu moja kisha akanipitisha katikati ya maji yale, maji yanayofika kwenye magoti.

Naye akaendelea kupima elfu moja na sasa akanipitisha katikati—maji yanayofika kiunoni.

5 Naye akaendelea kupima elfu moja. Kilikuwa kijito ambacho sikuweza kupita katikati, kwa maana maji hayo yalikuwa yameinuka juu, maji ya mtu kuweza kuogelea, kijito ambacho hakingeweza kupitwa katikati.

6 Ndipo akaniambia: "Je, umeona hili, Ee mwana wa binadamu?"

Kisha akanitembeza na kunirudisha kwenye ukingo wa kijito hicho. **7** Niliporudi, kumbe, tazama! kwenye ukingo wa kijito hicho kulikuwa na miti mingi sana, upande huu na upande ule.[b] **8** Naye akaendelea kuniambia: "Maji haya yanaenda eneo la mashariki nayo yatakwenda chini kupitia Araba.[c] Nayo yatakuja baharini.[d] Yanapoletwa katika bahari yenyewe,[e] maji yake kwa kweli huponywa pia. **9** Na itakuwa kwamba kila nafsi hai ambayo huzaana kwa wingi,[f] kila mahali ambapo huja kijito hicho kilichoongezeka ukubwa wake mara mbili, itapata uzima. Na itatukia kwamba kutakuwako samaki

wengi sana, kwa sababu hapo ndipo maji hayo hakika yataingia, nayo maji ya bahari yataponywa,[a] na kila kitu kitakuwa hai mahali ambapo kijito hicho kitafika.

10 "Na itatukia kwamba wavuvi watasimama kando yake kutoka En-gedi[b] mpaka Eneglaimu. Kutakuwa na uwanja wa kukaushia nyavu za kukokota. Kulingana na aina zake, samaki wao watakuwa wengi sana, kama samaki wa ile Bahari Kuu.[c]

11 "Kuna mahali pake penye majimaji na penye matope, napo hapataponywa.[d] Hakika pataachiwa chumvi.[e]

12 "Na kando ya kijito hicho, kando ya ukingo upande huu na upande ule, kutatokea kila namna ya miti kwa ajili ya chakula.[f] Majani yake hayatakauka,[g] wala matunda yake hayataharibiwa.[h] Kila mwezi itazaa matunda mapya, kwa sababu maji yake—yanatoka katika patakatifu penyewe.[i] Nayo matunda yake yatakuwa chakula na majani yake yatakuwa maponyo."[j]

13 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi: "Hili ndilo eneo ambalo mtajigawia kuwa urithi wa nchi ya makabila kumi na mawili ya Israeli, kukiwa na mafungu mawili ya shamba kwa Yosefu.[k] **14** Nanyi mtairithi, kila mmoja sawa na ndugu yake, nchi ambayo niliinua mkono wangu katika kiapo[l] kwamba nitawapa mababu zenu;[m] na nchi hiyo itawaangukia ninyi kwa kura ili kuwa urithi.[n]

15 "Na huu ndio mpaka wa nchi kuelekea upande wa kaskazini, kutoka Bahari Kuu kupitia njia ya kwenda Hethloni,[a] mtu anapoingia Sedadi,[b] **16** Hamathi,[c] Berotha,[d] Sibraimu, ulio katikati ya mpaka wa Damasko[e] na mpaka wa Hamathi; Haser-hatikoni, ulio kuelekea upande wa mpaka wa Haurani.[f] **17** Nao mpaka kutoka baharini utakuwa Hasar-enoni,[g] mpaka wa Damasko na kaskazini—kuelekea kaskazini, na mpaka wa Hamathi.[h] Huo ndio upande wa kaskazini.

18 "Na upande wa mashariki ni kutoka katikati ya Haurani[i] na Damasko[j] na katikati ya Gileadi[k] na nchi ya Israeli; Yordani,[l] kutoka katika mpaka wa bahari upande wa mashariki mtapima. Huo ndio upande wa mashariki.

19 "Na upande wa kusini ni kuelekea kusini, kutoka Tamari[m] mpaka maji ya Meribath-kadeshi,[n] bonde la mto[o] mpaka ile Bahari Kuu. Huo ndio upande wa kusini, kuelekea Negebu.

20 "Na upande wa magharibi ni ile Bahari Kuu, kutoka katika mpaka ulio mbele moja kwa moja hadi kuingia ndani huko Hamathi.[p] Huo ndio upande wa magharibi."

21 "Nanyi mtajigawia nchi hii, yale makabila kumi na mawili ya Israeli. **22** Na itatukia kwamba mtajigawia wenyewe iwe urithi[q] kwenu na kwa wakaaji wageni wanaokaa wakiwa wageni katikati yenu,[r] ambao wamezaa wana katikati yenu. Nao watakuwa kwenu kama mwenyeji katikati ya wana wa Israeli. Pamoja nanyi wataanguka katika urithi kwa kura katikati ya makabila ya

SURA 47
a Zb 103:3
b Yos 15:62
2Nya 20:2
c Hes 34:6
Yos 23:4
Eze 48:28
d Ebr 10:26
Ufu 22:11
e Kum 29:23
Zb 107:34
Yer 17:6
f Eze 47:7
g Zb 1:3
h Yer 17:8
i Eze 47:1
Ufu 22:1
j Ufu 22:2
k Mwa 48:5
1Nya 5:1
Eze 48:5
l Mwa 26:3
Hes 14:16
m Mwa 28:13
Eze 20:42
n Met 16:33
Eze 48:29

Safu ya 2
a Eze 48:1
b Hes 34:8
c Hes 13:21
d 2Sa 8:8
e Mwa 14:15
f Eze 47:18
g Hes 34:9
h Eze 48:1
i Eze 47:16
j 2Sa 8:5
k Mwa 31:23
Hes 32:1
Amu 10:8
l Mwa 13:10
m Eze 48:28
n Hes 20:13
Kum 32:51
Zb 81:7
o 2Fa 24:7
Eze 48:28
p Yos 13:5
Eze 48:28
q Eze 47:13
r Ro 10:12
Ga 3:8
Ufu 7:9

Israeli.[a] **23** Na itatukia kwamba katika kabila ambalo mkaaji mgeni anakaa akiwa mgeni, hapo ndipo mtakapompa urithi wake," asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

48 "Na haya ndiyo majina ya makabila hayo. Kutoka upande wa kaskazini, upande wa njia ya Hethloni[b] hadi kuingia ndani huko Hamathi,[c] Hasar-enani,[d] mpaka wa Damasko kuelekea kaskazini, upande wa Hamathi; nayo itakuwa na mpaka wa mashariki na wa magharibi, Dani[e] fungu moja. **2** Na kwenye mpaka wa Dani, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Asheri[f] moja. **3** Na kwenye mpaka wa Asheri, kutoka mpaka wa mashariki hata kwenye mpaka wa magharibi, Naftali[g] moja. **4** Na kwenye mpaka wa Naftali, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Manase[h] moja. **5** Na kwenye mpaka wa Manase, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Efraimu[i] moja. **6** Na kwenye mpaka wa Efraimu, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Rubeni[j] moja. **7** Na kwenye mpaka wa Rubeni, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Yuda[k] moja. **8** Na kwenye mpaka wa Yuda, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, mchango ambao ninyi mnapaswa kutoa unapaswa kuwa na upana wa mikono 25,000,[l] na urefu kulingana na moja la yale mafungu kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi.

SURA 47
a Kol 3:11

SURA 48
b Eze 47:15
c Hes 34:8
d Eze 47:17
e Mwa 30:6
f Mwa 30:13 Yos 19:24
g Mwa 30:8 Yos 19:32
h Mwa 41:51 Mwa 48:14 Yos 13:29
i Mwa 48:5 Yos 16:5 Yos 17:17
j Mwa 49:3
k Mwa 29:35 Yos 15:1 Yos 19:9
l Eze 45:1

Safu ya 2
a Ufu 21:3
b Hes 35:2 Yos 21:3 Eze 45:4
c Eze 48:8
d Eze 40:46 Eze 43:19 Eze 44:15
e Yer 23:11 Eze 22:26 Eze 44:10
f Eze 45:4
g Kum 12:19
h Eze 45:3
i Law 27:21

Napo patakatifu patakuwa katikati yake.[a]

9 "Kwa habari ya mchango ambao mnapaswa kumtolea Yehova, urefu utakuwa mikono 25,000 na upana mikono 10,000. **10** Na kwa habari yake kutakuwako mchango mtakatifu kwa ajili ya makuhani,[b] upande wa kaskazini mikono 25,000, na upande wa magharibi upana wa mikono 10,000, na upande wa mashariki upana wa mikono 10,000, na upande wa kusini urefu wa mikono 25,000. Na patakatifu pa Yehova patakuwa katikati yake.[c] **11** Patakuwa kwa ajili ya makuhani, waliotakaswa kutoka kwa wana wa Sadoki,[d] ambao waliutunza wajibu kunielekea mimi, ambao hawakuenda mbali wakati ambapo wana wa Israeli walienda huku na huku, kama vile Walawi walivyoenda huku na huku.[e] **12** Nao watakuwa na mchango kutoka katika mchango wa hiyo nchi ukiwa kitu kitakatifu zaidi, kwenye mpaka wa Walawi.[f]

13 "Na Walawi watakuwa na fungu,[g] karibu kabisa na eneo la makuhani, lenye urefu wa mikono 25,000, na upana wa mikono 10,000; urefu wote ukiwa 25,000, na upana ukiwa 10,000.[h] **14** Nao hawapaswi kuuza sehemu yoyote kati ya hiyo, wala mtu hapaswi kubadilishana, wala mtu hapaswi kuacha sehemu bora zaidi ya nchi itoke kwao; kwa maana hicho ni kitu kitakatifu kwa Yehova.[i]

15 "Kwa habari ya ile mikono 5,000 inayobaki katika upa-

na kandokando ya ile mikono 25,000, ni kitu najisi cha jiji,[a] kiwe makao na kiwe uwanja wa malisho. Nalo jiji litakuwa katikati yake.[b] **16** Na hivi ndivyo vipimo vya jiji: mpaka wa kaskazini mikono 4,500, na mpaka wa kusini 4,500, na mpaka wa mashariki 4,500, na mpaka wa magharibi 4,500. **17** Na jiji litakuwa na uwanja wa malisho,[c] upande wa kaskazini mikono 250, na upande wa kusini 250, na upande wa mashariki 250, na upande wa magharibi 250.

18 "Na kitakachobaki katika urefu kitalingana kabisa na mchango mtakatifu,[d] mikono 10,000 upande wa mashariki, na 10,000 upande wa magharibi; napo patalingana kabisa na mchango mtakatifu, na mazao yake yatakuwa kwa ajili ya mkate wa wale wanaotumikia jiji.[e] **19** Na wale wanaotumikia jiji kutoka katika makabila yote ya Israeli watapalima.[f]

20 "Mchango mzima ni mikono 25,000 urefu kwa 25,000 upana. Mtachanga sehemu iliyo mraba iwe mchango mtakatifu pamoja na miliki ya jiji.

21 "Na sehemu iliyobaki itakuwa ya mkuu,[g] upande huu na upande ule wa mchango mtakatifu na wa miliki ya jiji,[h] kando ya mikono 25,000 ya mchango mtakatifu kuelekea mpaka wa mashariki; na upande wa magharibi kando ya mikono 25,000 kuelekea mpaka wa magharibi.[i] Kama yalivyo mafungu hayo, ndivyo itakavyokuwa kwa ajili ya mkuu. Na mchango mtakatifu na patakatifu pa ile Nyumba patakuwa katikati yake.

22 "Nayo miliki ya Walawi na miliki ya jiji, itakuwa katikati ya miliki ya mkuu. Katikati ya mpaka wa Yuda[a] na mpaka wa Benyamini itakuwa ya mkuu.

23 "Nayo yale makabila mengine, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Benyamini[b] fungu moja. **24** Na kando ya mpaka wa Benyamini, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Simeoni[c] moja. **25** Na kando ya mpaka wa Simeoni, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Isakari[d] moja. **26** Na kando ya mpaka wa Isakari, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Zabuloni[e] moja. **27** Na kando ya mpaka wa Zabuloni, kutoka mpaka wa mashariki hadi mpaka wa magharibi, Gadi[f] moja. **28** Na kando ya mpaka wa Gadi, hadi mpaka wa kusini, litakuwa kuelekea kusini; nao mpaka utakuwa kutoka Tamari[g] hadi maji ya Meribath-kadeshi,[h] hadi kwenye bonde la mto,[i] hadi kwenye ile Bahari Kuu.[j]

29 "Hii itakuwa nchi ambayo mtafanya iangukie makabila ya Israeli kwa kura iwe urithi,[k] na hayo yatakuwa mafungu yao,"[l] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova.

30 "Na haya yatakuwa malango ya kutokea ya jiji: Kwenye mpaka wa kaskazini, kipimo kitakuwa mikono 4,500.[m]

31 "Na malango ya jiji yatakuwa kulingana na makabila ya

SURA 48

a Eze 45:6
b Eze 48:35
c Eze 45:2
d Eze 45:1
e 2Fa 25:3
f Eze 45:6
g Zb 45:16
Isa 32:1
h Eze 45:7
i Eze 48:8

Safu ya 2

a Eze 48:8
b Mwa 35:18
Yos 18:21
c Mwa 49:5
Yos 19:1
d Mwa 49:14
Yos 19:17
e Mwa 49:13
Yos 19:10
f Mwa 30:11
Mwa 49:19
g Eze 47:19
h Hes 20:13
i Mwa 15:18
j Eze 47:15
k Hes 34:2
Hes 34:13
Yos 14:2
l Eze 47:13
m Eze 48:16

Israeli, malango matatu yakiwa upande wa kaskazini, lango la Rubeni, moja; lango la Yuda, moja; lango la Lawi, moja.

32 "Na kwenye mpaka wa mashariki kutakuwa mikono 4,500, na malango matatu, naam, lango la Yosefu, moja; lango la Benyamini, moja; lango la Dani, moja.

33 "Na mpaka wa kusini utakuwa mikono 4,500 kipimo chake, ukiwa na malango matatu, lango la Simeoni, moja; lango la Isakari, moja; lango la Zabuloni, moja.

34 "Mpaka wa magharibi utakuwa mikono 4,500, kukiwa na malango matatu, lango la Gadi, moja; lango la Asheri, moja; lango la Naftali, moja.

35 "Kuzunguka pande zote kutakuwa mikono 18,000; na jina la jiji kutoka siku hiyo na kuendelea litakuwa, Yehova Mwenyewe Yupo Hapo."[a]

Safu ya 2

SURA 48
a Yer 3:17
Yoe 3:21
Zek 2:10

DANIELI

1 Katika mwaka wa tatu wa ufalme wa Yehoyakimu[a] mfalme wa Yuda, Nebukadneza mfalme wa Babiloni alikuja Yerusalemu na kulizingira.[b] **2** Baada ya muda Yehova akamtia Yehoyakimu mfalme wa Yuda[c] mkononi mwake, pamoja na sehemu ya vyombo[d] vya nyumba ya Mungu wa kweli, naye akavileta katika nchi ya Shinari[e] nyumbani kwa mungu wake; akaleta vyombo hivyo kwenye nyumba ya hazina ya mungu wake.[f]

3 Ndipo mfalme akamwambia Ashpenazi ofisa mkuu wa makao yake ya kifalme[g] awalete baadhi ya wana wa Israeli na wa uzao wa kifalme na wa watu wenye vyeo,[h] **4** watoto ambao hawakuwa na kasoro yoyote,[i] bali wenye sura nzuri, wenye ufahamu katika hekima yote, wenye ujuzi,[j] wenye utambuzi kuhusu mambo yanayojulikana,[k] ambao pia walikuwa na uwezo wa kusimama katika jumba la mfalme;[a] na kuwafundisha maandishi na lugha ya Wakaldayo. **5** Tena mfalme akawawekea posho ya kila siku katika vyakula vitamu[b] vya mfalme na katika divai yake ya kunywa, ili kuwalisha miaka mitatu, ndipo mwishowe wasimame mbele ya mfalme.

6 Basi kati yao walikuwa baadhi ya wana wa Yuda, Danieli,[c] Hanania, Mishaeli na Azaria.[d] **7** Naye ofisa mkuu wa makao ya mfalme akawapa majina.[e] Basi akamwita Danieli jina Belteshaza;[f] Hanania akamwita Shadraki; Mishaeli akamwita Meshaki; naye Azaria akamwita Abednego.[g]

8 Lakini Danieli aliazimia moyoni mwake kwamba hatajitia unajisi[h] kwa vyakula vitamu vya mfalme wala kwa divai yake ya kunywa. Naye akazidi kumwomba ofisa mkuu wa makao ya mfalme ili asijitie unajisi.[i] **9** Basi Mungu wa kweli akampa Danieli fadhili ze-

SURA 1
a 2Nya 36:4
Yer 22:18
Yer 36:30
b Kum 28:49
2Fa 24:1
2Nya 36:6
c Zb 106:41
Isa 42:24
d 2Nya 36:7
Yer 27:19
e Mwa 10:10
Mwa 11:2
f Ezr 1:7
g Da 1:11
h 2Fa 20:18
Isa 39:7
i 2Sa 14:25
Wim 4:7
j Mhu 7:19
Da 1:20
Da 2:20
Da 5:11
k Da 1:17

Safu ya 2
a Met 22:29
b 1Fa 4:22
Da 1:15
c Da 2:48
Da 5:13
Da 5:29
d Da 2:17
e Mwa 41:45
2Fa 23:34
2Fa 24:17
f Da 4:8
Da 5:12
g Da 2:49
Da 3:12
Da 3:28
h Law 11:4
Law 11:13
Law 17:12
i Law 11:47
Zb 119:2
Eze 4:13

nye upendo na rehema mbele
ya yule ofisa mkuu wa makao
ya mfalme.[a] **10** Ndipo huyo
ofisa mkuu wa makao ya
mfalme akamwambia Danieli:
"Mimi namwogopa bwana wa-
ngu mfalme, ambaye ameagi-
za chakula chenu na kinywa-
ji chenu.[b] Kwa nini, basi, aone
nyuso zenu zina sura ya hu-
zuni zikilinganishwa na wa-
toto ambao wana umri kama
wenu, na kwa nini mkifanye
kichwa changu kiwe na hatia
mbele ya mfalme?" **11** La-
kini Danieli akamwambia mli-
nzi ambaye ofisa mkuu wa ma-
kao ya mfalme[c] alikuwa ame-
mweka juu ya Danieli, Hana-
nia, Mishaeli na Azaria:
12 "Tafadhali, uwajaribu wa-
tumishi wako kwa siku kumi,
na watupe mboga za majani[d]
tule na maji tunywe; **13** ki-
sha sura zetu na sura za wale
watoto wanaokula vyakula vi-
tamu vya mfalme zionekane
mbele yako, nawe uwatendee
watumishi wako kulingana na
unavyoona."
14 Mwishowe akawasikiliza
kwa jambo hilo, akawajaribu
kwa siku kumi. **15** Na mwi-
shoni mwa zile siku kumi, sura
zao zikaonekana kuwa bora
na zilizonenepa kuliko za wale
watoto wote waliokuwa wa-
kila vyakula vitamu vya mfa-
lme.[e] **16** Kwa hiyo yule mli-
nzi akaendelea kuondoa vya-
kula vyao vitamu na divai yao
ya kunywa, akawapa mboga
za majani.[f] **17** Basi Mungu
wa kweli akawapa watoto hao
wanne ujuzi na ufahamu kati-
ka maandishi na hekima yote;[g]
naye Danieli alikuwa akielewa
maono na ndoto za aina zote.[h]

SURA 1
a 1Fa 8:50
Zb 106:46
Met 16:7
b Met 29:25
c Da 1:3
d Mwa 1:29
e Met 10:22
f Da 1:12
g Zb 119:98
Met 2:6
Mhu 2:26
Isa 28:26
h Hes 12:6
Da 1:20
Da 4:9
Da 5:11

Safu ya 2
a Da 1:5
b Da 1:6
c Met 22:29
d Zb 119:100
Met 4:7
Met 4:8
e Kut 7:11
f Da 2:2
Da 4:7
Da 5:8
g Da 6:28
Da 10:1

SURA 2
h Mwa 40:5
i Mwa 41:8
Da 4:5
j Da 1:20
k Isa 19:3
Isa 47:13
Da 2:10
Da 2:27
Da 4:7
Da 5:7
l Ezr 4:7
Isa 36:11
m 1Sa 10:24
Ne 2:3
Da 3:9
n Mwa 41:8

18 Basi mwishoni mwa siku
ambazo mfalme alikuwa ame-
sema waletwe ndani,[a] ofisa
mkuu wa makao ya mfalme pia
akawaleta ndani, mbele ya Ne-
bukadneza. **19** Naye mfalme
akaanza kusema nao, na kati
yao wote hakupatikana ye-
yote aliye kama Danieli, Ha-
nania, Mishaeli na Azaria;[b] nao
wakaendelea kusimama mbe-
le ya mfalme.[c] **20** Na kati-
ka kila jambo la hekima na
la uelewaji[d] alilowauliza mfa-
lme, akawaona kuwa bora
mara kumi kuliko makuhani[e]
wote wenye kufanya uchawi
na wafanya-mazingaombwe[f]
waliokuwa katika ufalme wake
wote. **21** Naye Danieli akae-
ndelea kudumu kufikia mwa-
ka wa kwanza wa Koreshi
mfalme.[g]

2 Na katika mwaka wa pili
wa ufalme wa Nebukadne-
za, Nebukadneza aliota ndo-
to;[h] na roho yake ikaanza ku-
hangaika,[i] usingizi wake uka-
toweka. **2** Basi mfalme aka-
agiza waitwe makuhani wote
wenye kufanya uchawi[j] na wa-
fanya-mazingaombwe na wa-
lozi na Wakaldayo ili wamwa-
mbie mfalme ndoto zake.[k] Nao
wakaingia na kusimama mbe-
le ya mfalme. **3** Ndipo mfa-
lme akawaambia: "Kuna ndoto
ambayo nimeota, na roho ya-
ngu imehangaika kwa kutaka
kuijua ndoto hiyo." **4** Basi
Wakaldayo wakasema na mfa-
lme katika lugha ya Kiara-
mu:[l] "Ee mfalme, uishi mpa-
ka wakati usio na kipimo.[m]
Waambie watumishi wako
ndoto hiyo, nasi tutaonyesha
tafsiri yake."[n]

5 Mfalme akajibu na kuwa-
ambia Wakaldayo: "Mimi na-
tangaza neno hili: Msiponijuli-
sha ndoto hiyo, na tafsiri yake,
mtakatwa vipande-vipande,[a]
na nyumba zenu zitageuzwa
kuwa vyoo vya watu wote.[b]
6 Bali mkionyesha ndoto hiyo
na tafsiri yake, mtapokea za-
wadi na tuzo na heshima ku-
bwa kutoka kwangu.[c] Basi nio-
nyesheni ndoto hiyo na tafsiri
yake."
7 Kisha wakajibu mara ya
pili na kusema: "Mfalme na awa-
ambie watumishi wake ndoto
hiyo, nasi tutaonyesha tafsiri
yake."
8 Mfalme akajibu na kuse-
ma: "Hakika mimi najua kwa-
mba mnajaribu kupata waka-
ti, kwa vile mmejua kuwa ni-
natangaza neno hili. **9** Kwa
kuwa msiponijulisha ndoto
hiyo, kuna hukumu moja[d] tu
juu yenu. Lakini mmekubalia-
na kusema mbele yangu uwo-
ngo na neno lenye kosa,[e] mpa-
ka wakati ubadilishwe. Basi
niambieni ndoto hiyo, nami ni-
tajua kwamba mnaweza kuo-
nyesha tafsiri yake."
10 Wakaldayo wakajibu mbe-
le ya mfalme, na kusema: "Ha-
kuna binadamu yeyote juu ya
nchi kavu anayeweza kuonye-
sha jambo hili la mfalme, kwa
vile hakuna mfalme mkuu wala
gavana ambaye amepata kuuli-
za jambo kama hili kutoka kwa
kuhani yeyote mwenye kufanya
uchawi, wala mfanya-mazingao-
mbwe wala Mkaldayo. **11** La-
kini jambo hili ambalo mfalme
anauliza ni gumu, wala hakuna
mtu mwingine yeyote anayewe-
za kulionyesha mbele ya mfa-
lme isipokuwa miungu,[f] ambao
makao yao hayako kamwe pa-
moja na wenye mwili wa nya-
ma."[a]
12 Kwa sababu hiyo mfalme
akakasirika na kuwa na
ghadhabu sana,[b] naye akaa-
giza watu wote wenye hekima
wa Babiloni waangamizwe.[c]
13 Nalo agizo likatolewa, na
watu wenye hekima wakawa
karibu kuuawa; nao wakamta-
futa Danieli na wenzake, ili
wauawe.
14 Ndipo wakati huo, kwa
shauri na akili,[d] Danieli akamzu-
ngumzia Arioko mkuu wa wa-
linzi wa mfalme, aliyekuwa ame-
enda kuwaua watu wenye he-
kima wa Babiloni. **15** Akamu-
uliza Arioko ofisa wa mfalme:
"Kwa nini mfalme ametoa agi-
zo kali namna hii?" Ndipo Ari-
oko akamjulisha Danieli ja-
mbo hilo.[e] **16** Basi Danieli
mwenyewe akaingia na kuom-
ba mfalme ampe wakati ma-
alumu ili amwonyeshe mfalme
tafsiri ile.[f]
17 Kisha Danieli akaenda
nyumbani kwake; naye aka-
wajulisha wenzake jambo hilo,
Hanania, Mishaeli na Azaria,
18 ili waombe rehema[g] kutoka
kwa Mungu wa mbinguni[h] ku-
husu siri hiyo,[i] kwamba Danie-
li na wenzake pamoja na wale
watu wengine wenye hekima
wa Babiloni wasiangamizwe.[j]
19 Ndipo Danieli akafunu-
liwa siri hiyo katika maono
ya usiku.[k] Basi Danieli aka-
mbariki[l] Mungu wa mbingu-
ni. **20** Danieli akajibu na ku-
sema: "Jina la Mungu na liba-
rikiwe[m] kutoka wakati usio
na kipimo mpaka wakati usio
na kipimo, maana hekima na

SURA 2
a Da 3:29
b 2Fa 10:27
Ezr 6:11
c Da 2:48
Da 5:7
Da 5:16
Da 5:29
d Da 2:5
e Met 12:19
f Da 2:23
Da 2:28
Da 2:47

Safu ya 2
a 2Nya 6:18
b Met 16:14
Met 19:12
Met 20:2
c Da 2:24
d Mhu 10:4
e Da 2:9
f Mwa 41:16
g Zb 116:5
h Zb 115:3
Zb 115:16
i Zb 50:15
Met 3:5
Mt 18:19
j Mwa 18:23
Mal 3:18
2Pe 2:9
k Hes 12:6
Ayu 33:15
Zb 25:14
Da 2:28
1Ko 2:11
l Zb 50:15
Zb 145:10
m 1Nya 29:20
Zb 34:1
Zb 72:18
Zb 113:2

nguvu ni zake.[a] **21** Naye anabadili nyakati na majira,[b] akiondoa wafalme na kuwasimamisha wafalme,[c] akiwapa hekima wenye hekima na kuwapa ujuzi wale wanaojua utambuzi.[d] **22** Yeye anafunua mambo mazito na yale yaliyofichwa,[e] akijua yaliyo katika giza;[f] nayo nuru[g] hukaa kwake. **23** Nami nakusifu wewe na kukuhimidi,[h] Ee Mungu wa mababu zangu, kwa maana umenipa mimi hekima[i] na nguvu. Na sasa umenijulisha tulilokuomba, kwa kuwa umetujulisha jambo lile la mfalme."[j]

24 Kwa sababu hiyo Danieli akaingia kwa Arioko,[k] ambaye mfalme alikuwa amemweka awaangamize watu wenye hekima wa Babiloni.[l] Akaenda, akamwambia hivi: "Usiangamize yeyote kati ya watu wenye hekima wa Babiloni. Nipeleke mbele ya mfalme,[m] nimwonyeshe mfalme ile tafsiri."

25 Ndipo Arioko akampeleka Danieli haraka-haraka mbele ya mfalme, akamwambia hivi: "Nimepata mwanamume mmoja kutoka kwa wahamishwa[n] wa Yuda anayeweza kumjulisha mfalme ile tafsiri." **26** Basi mfalme akajibu na kumwambia Danieli, ambaye jina lake aliitwa Belteshaza:[o] "Je, una uwezo wa kutosha kuniambia ndoto niliyoona, na tafsiri yake?"[p] **27** Danieli akajibu mbele ya mfalme na kusema: "Siri ambayo mfalme anauliza, watu wenye hekima, wala wafanya-mazingaombwe, wala makuhani wenye kufanya uchawi wala wanajimu hawawezi kumwonyesha mfalme.[a] **28** Hata hivyo, kuna Mungu mbinguni ambaye ni Mfunuaji wa siri,[b] naye amemjulisha Mfalme Nebukadneza mambo yatakayotokea katika siku za mwisho.[c] Ndoto yako na maono ya kichwa chako kitandani mwako ndiyo haya:

29 "Wewe, Ee mfalme, ukiwa kitandani[d] mwako mawazo yako yalikuja kuhusu mambo yatakayotokea baada ya haya, na Aliye Mfunuaji wa siri amekujulisha mambo yatakayotokea.[e] **30** Lakini mimi sikufunuliwa siri hii kwa sababu nina hekima ndani yangu kuliko watu wengine walio hai,[f] bali kusudi mfalme mwenyewe aambiwe tafsiri, upate kujua mawazo ya moyo wako.[g]

31 "Wewe, Ee mfalme, ulikuwa ukiangalia, na tazama! sanamu fulani kubwa sana. Sanamu hiyo, iliyokuwa kubwa na ambayo mwangaza wake ulikuwa usio wa kawaida, ilikuwa imesimama mbele yako, na sura yake ilitia hofu. **32** Na sanamu hiyo ilikuwa na kichwa cha dhahabu safi,[h] kifua na mikono ya fedha,[i] tumbo na mapaja ya shaba,[j] **33** miguu ya chuma,[k] nyayo zake zilikuwa sehemu moja chuma na sehemu nyingine udongo uliofinyangwa.[l] **34** Uliendelea kutazama mpaka jiwe likakatwa bila kutumia mikono,[m] nalo likaipiga sanamu hiyo juu ya nyayo zake za chuma na za udongo uliofinyangwa, likaziponda.[n] **35** Wakati huo kile chuma, ule udongo uliofinyangwa, ile shaba, ile fedha na ile dhahabu, zote pamoja,

SURA 2

a 1Nya 29:11
Ayu 12:13
Zb 147:5
Yer 32:18
b Isa 60:22
Da 7:25
Mdo 1:7
c 1Sa 2:7
Zb 75:7
Met 8:15
Yer 27:5
Da 4:17
d Met 2:6
Mhu 2:26
Efe 1:17
Yak 1:5
e Ayu 12:22
Yer 33:3
1Ko 2:10
f Zb 139:12
Ebr 4:13
g Zb 36:9
Zb 112:4
1Yo 1:5
h Zb 145:3
Da 2:28
i Mhu 7:19
Da 1:17
j Amo 3:7
k Da 2:15
l Da 2:12
m Da 1:19
Da 2:16
n Ne 7:6
Da 1:6
Da 6:13
o Da 1:7
Da 4:8
Da 4:19
Da 5:12
p Da 4:18
Da 5:16

Safu ya 2

a Isa 47:12
Da 2:10
b Mwa 40:8
Da 1:17
c Da 10:14
d Ayu 33:15
e Ufu 4:1
f Mdo 3:12
g Da 2:47
h Yer 51:7
Da 2:38
Da 4:22
Da 7:4
i Da 2:39
Da 5:28
Da 7:5
Da 8:3
j Da 7:6
Da 8:5
k Da 2:40
Da 7:7
Da 7:19
l Da 2:41
m Da 2:45
Da 7:14
Da 7:27
Ufu 12:5
n Da 2:44
Ufu 11:15

zilipondwa na kuwa kama makapi yanayotoka kwenye uwanja wa kupuria wa wakati wa kiangazi,[a] kisha upepo ukazipeleka mbali hivi kwamba alama zake hazikuonekana hata kidogo.[b] Na lile jiwe lililoipiga sanamu ile likawa mlima mkubwa, na kuijaza dunia yote.[c]

36 "Hii ndiyo ndoto ile, nasi tutaisema tafsiri yake mbele ya mfalme.[d] **37** Wewe, Ee mfalme, uliye mfalme wa wafalme, wewe ambaye Mungu wa mbinguni amekupa ufalme,[e] uwezo, na nguvu na heshima, **38** na amekupa mkononi mwako,[f] popote pale ambapo wana wa binadamu hukaa, wanyama wa mwituni na viumbe vya mbinguni vyenye mabawa, na amekufanya kuwa mtawala juu ya vyote hivyo. Wewe ndiye kile kichwa cha dhahabu.[g]

39 "Na baada yako utasimama ufalme[h] mwingine ulio mdogo kwako;[i] na ufalme mwingine, wa tatu, wa shaba, ambao utaitawala dunia yote.[j]

40 "Ufalme wa nne[k] nao utakuwa wenye nguvu kama chuma.[l] Kwa vile chuma huponda na kusaga vitu vingine vyote, basi, kama chuma ambacho huvunja-vunja, huo utaziponda na kuzivunja-vunja hizi nyingine zote.[m]

41 "Na kama vile ulivyoona kuwa nyayo na vidole vya miguu vilikuwa sehemu moja ni udongo uliofinyangwa na nyingine ni chuma,[n] ufalme huo utakuwa umegawanyika,[o] lakini ugumu fulani wa chuma utakuwa ndani yake, kama vile ulivyoona chuma kimechanganyikana na udongo mbichi.[p]

SURA 2

a Zb 1:4
b Zb 37:10
Ufu 20:11
c Zb 22:27
Isa 11:9
d Da 2:23
e Yer 28:14
Da 5:18
f Yer 27:5
g Da 2:32
Da 4:21
h Isa 45:1
Yer 51:28
Da 5:28
Da 11:2
i Da 8:20
j Da 7:6
Da 8:21
Da 10:20
Da 11:3
k Da 2:33
l Da 7:19
Da 7:23
Yoh 11:48
m Da 7:7
n Da 2:33
o Mt 12:25
p Da 2:34

Safu ya 2

a Da 7:12
Ufu 17:12
b Ezr 1:2
Zb 115:3
Zb 115:16
c Mwa 49:10
Zb 2:6
Mt 6:10
Lu 22:29
Yoh 18:36
Ufu 11:15
Ufu 20:6
d 2Sa 7:13
Isa 9:7
Eze 37:25
Da 7:14
Mik 4:7
Ufu 11:15
e Da 4:17
Da 7:27
f Zb 2:9
Zb 110:5
Isa 60:12
Da 11:45
Ufu 19:15
g Da 4:3
Da 4:34
Lu 1:33
h Isa 28:16
Da 2:34
i Da 2:35
j 2Sa 7:22
Zb 96:4
Zb 145:3
Yer 32:18
k Mwa 41:28
Da 2:28
l Isa 14:24
Isa 44:26
m Ezr 6:10
n Kum 32:39
Zb 136:2
Da 11:36
1Ko 8:5
o Kum 10:17
Zb 136:3
p Mwa 41:39
Da 1:17
Da 2:28
Da 4:9
Amo 3:7

42 Na kuhusu vidole vya miguu ambavyo vilikuwa sehemu moja ni chuma na nyingine ni udongo uliofinyangwa, sehemu moja ya ufalme huo itakuwa yenye nguvu na nyingine itakuwa dhaifu. **43** Na kama ulivyoona chuma kimechanganyikana na udongo mbichi, watachanganyikana na uzao wa wanadamu; lakini hawatashikamana pamoja, huyu na yule, kama vile chuma kisivyochanganyikana na udongo uliofinyangwa.

44 "Na katika siku za wafalme hao,[a] Mungu wa mbinguni[b] atausimamisha ufalme[c] ambao hautaharibiwa kamwe.[d] Na ufalme huo hautapewa watu wengine wowote.[e] Utazivunja na kuzikomesha falme hizi zote,[f] nao utasimama mpaka wakati usio na kipimo;[g] **45** kama vile ulivyoona kwamba kutoka katika mlima jiwe lilikatwa bila kutumia mikono,[h] na kwamba liliponda kile chuma, ile shaba, ule udongo uliofinyangwa, ile fedha na ile dhahabu.[i] Mungu Mkuu[j] mwenyewe amemjulisha mfalme mambo yatakayotokea baada ya haya.[k] Na ndoto hiyo ni yenye kutegemeka, na tafsiri yake ni yenye kuaminika."[l]

46 Wakati huo Mfalme Nebukadneza akaanguka kifudifudi, akampa Danieli heshima kubwa, na kusema apewe tuzo na kutolewa uvumba.[m] **47** Mfalme akamwambia Danieli: "Kwa kweli Mungu wenu ni Mungu wa miungu[n] na Bwana wa wafalme[o] na Mfunuaji wa siri, kwa sababu uliweza kufunua siri hii."[p] **48** Basi

mfalme akamfanya Danieli
kuwa mtu mkuu,[a] akampa za-
wadi nyingi kubwa, naye
akamfanya kuwa mtawala juu
ya wilaya yote ya utawala ya
Babiloni na mkuu wa mana-
ibu wa maliwali juu ya watu
wote wenye hekima wa Babilo-
ni.[b] **49** Naye Danieli akatoa
ombi kwa mfalme, naye akawe-
ka Shadraki, Meshaki na Abe-
dnego[c] juu ya usimamizi wa wi-
laya ya utawala ya Babiloni, la-
kini Danieli akawa katika ma-
kao ya mfalme.[d]

3 Mfalme Nebukadneza ali-
tengeneza sanamu[e] ya
dhahabu, ambayo urefu wake
ulikuwa mikono 60 na upana
wake mikono 6. Akaisimamis-
ha katika nchi tambarare ya
Dura katika wilaya ya utawala
ya Babiloni.[f] **2** Naye Mfalme
Nebukadneza akatuma watu
wawakusanye maliwali, mana-
ibu wa maliwali[g] na magavana,
washauri, waweka-hazina, wa-
amuzi, mahakimu watekeleza-
sheria[h] na wasimamizi wote wa
wilaya za utawala waje kwenye
mzinduo[i] wa sanamu ambayo
Mfalme Nebukadneza alikuwa
ameisimamisha.
3 Ndipo maliwali,[j] manaibu
wa maliwali na magavana, wa-
shauri, waweka-hazina, wa-
amuzi, mahakimu watekeleza-
sheria na wasimamizi wa wila-
ya zote za utawala wakaanza
kujikusanya kwa ajili ya ku-
zinduliwa kwa sanamu amba-
yo Mfalme Nebukadneza aliku-
wa ameisimamisha, wakawa
wanasimama mbele ya sana-
mu ambayo Nebukadneza ali-
kuwa ameisimamisha. **4** Na
mtangazaji[k] akapaaza sauti:

SURA 2
a Da 5:16
b Da 2:6
Da 5:29
c Da 1:7
d Est 2:19
Est 3:2
Yer 39:3
Amo 5:15

SURA 3
e Isa 40:19
Mdo 17:29
1Ko 8:4
f Est 1:1
Da 2:48
g Da 6:7
h Ezr 7:25
Mdo 16:20
i Ezr 6:16
j Est 8:9
Da 6:1
k Da 5:29

Safu ya 2
a Est 8:9
Da 4:1
b Da 3:10
Da 3:15
c Kut 20:5
Mt 4:9
d Da 4:19
Da 4:33
e Yer 29:22
Da 3:11
Da 3:17
Da 3:26
Ufu 13:15
f Yer 51:7
Mdo 14:16
g Da 3:12
h Ne 2:3
Da 2:4
Da 5:10
i Ayu 21:12
Da 3:5
Da 3:15
j Da 3:6

"Enyi vikundi vya watu, vya
mataifa na lugha mnaamriwa[a]
5 kwamba, wakati mtakaposi-
kia sauti ya baragumu, zuma-
ri, zeze, kinubi chenye pembe
tatu, kinanda, zumari-tete na
aina zote za vyombo vya mu-
ziki,[b] mwanguke chini na
kuiabudu sanamu ya dhahabu
ambayo Mfalme Nebukadne-
za ameisimamisha. **6** Na ye-
yote ambaye hataanguka chi-
ni na kuabudu[c] atatupwa wa-
kati huohuo[d] ndani ya tanu-
ru inayowaka moto."[e] **7** Kwa
hiyo, wakati ambapo vikundi
vyote vya watu vilisikia sau-
ti ya baragumu, zumari, zeze,
kinubi chenye pembe tatu, ki-
nanda na aina zote za vyombo
vya muziki, vikundi vyote vya
watu,[f] vya mataifa na lugha vi-
kaanguka chini na kuiabudu
sanamu ya dhahabu ambayo
Mfalme Nebukadneza alikuwa
ameisimamisha.
8 Kwa hiyo, wakati huohuo
Wakaldayo fulani wakakari-
bia na kuwashtaki Wayahudi.[g]
9 Wakajibu na kumwambia
Mfalme Nebukadneza: "Ee
mfalme, uishi mpaka nyaka-
ti zisizo na kipimo.[h] **10** Wewe
mwenyewe, Ee mfalme, ulitoa
amri kwamba kila mtu anaye-
sikia sauti ya baragumu, zu-
mari, zeze, kinubi chenye pe-
mbe tatu, kinanda, na zuma-
ri-tete na aina zote za vyombo
vya muziki,[i] aanguke chini na
kuabudu ile sanamu ya dha-
habu; **11** na kwamba yeyote
ambaye haanguki chini na ku-
abudu atupwe ndani ya tanuru
inayowaka moto.[j] **12** Kuna
Wayahudi fulani ambao uliwe-
ka juu ya usimamizi wa wilaya

ya utawala ya Babiloni,[a] Shadraki, Meshaki na Abednego; wanaume hao hawakukujali wewe, Ee mfalme, hawaitumikii miungu yako mwenyewe, wala sanamu ya dhahabu ambayo umeisimamisha hawaiabudu."[b]

13 Ndipo Nebukadneza, akiwa na ghadhabu na hasira,[c] akasema Shadraki, Meshaki na Abednego waletwe ndani.[d] Basi wanaume hao wakaletwa mbele ya mfalme. **14** Nebukadneza akawauliza: "Je, ni kweli, enyi Shadraki, Meshaki na Abednego, kwamba ninyi hamwitumikii miungu yangu,[e] wala sanamu ya dhahabu ambayo nimeisimamisha hamwiabudu?[f] **15** Basi sasa ikiwa mko tayari ili mnaposikia sauti ya baragumu, zumari, zeze, kinubi chenye pembe tatu, kinanda, zumari-tete na aina zote za vyombo vya muziki,[g] mwanguke chini na kuiabudu sanamu ambayo nimeitengeneza, ni vema. Lakini msipoabudu, mtatupwa wakati huohuo ndani ya tanuru inayowaka moto. Na ni mungu gani huyo anayeweza kuwaokoa ninyi kutoka mikononi mwangu?"[h]

16 Shadraki, Meshaki na Abednego wakajibu, nao wakamwambia mfalme: "Ee Nebukadneza, si lazima tukujibu neno lolote kuhusu jambo hili.[i] **17** Kama ni hivyo, Mungu ambaye tunamtumikia anaweza kutuokoa. Yeye atatuokoa[j] kutoka katika tanuru inayowaka moto na kutoka mkononi mwako, Ee mfalme. **18** Lakini kama sivyo, ujue hivi, Ee mfalme, kwamba sisi hatuitumikii miungu yako, na sanamu ambayo umeisimamisha hatutaiabudu."[a]

19 Ndipo Nebukadneza akajaa ghadhabu, na sura ya uso wake ikabadilika juu ya Shadraki, Meshaki na Abednego. Akasema kwamba tanuru itiwe moto mara saba kuliko iliyokuwa kawaida kuitia moto. **20** Naye akawaambia wanaume fulani wenye nguvu[b] waliokuwa katika jeshi lake wawafunge Shadraki, Meshaki na Abednego, ili wawatupe ndani ya ile tanuru inayowaka moto.[c]

21 Ndipo wanaume hao wakafungwa wakiwa na nguo zao za kujitanda, mavazi yao na kofia zao na nguo zao nyingine, wakatupwa ndani ya ile tanuru inayowaka moto. **22** Na kwa kuwa neno la mfalme lilikuwa kali na tanuru ilitiwa moto kupita kiasi, hao wanaume ambao waliwachukua Shadraki, Meshaki na Abednego ndio waliouawa na mwali wa moto. **23** Lakini hao wanaume wengine watatu, Shadraki, Meshaki na Abednego, wakaanguka wakiwa wamefungwa katikati ya ile tanuru inayowaka moto.[d]

24 Ndipo Mfalme Nebukadneza akaogopa, akasimama haraka. Akawauliza maofisa wake wakuu wa kifalme: "Je, hatukutupa wanaume watatu ndani ya moto wakiwa wamefungwa?"[e] Wakajibu na kumwambia mfalme: "Ndiyo, Ee mfalme." **25** Akajibu na kusema: "Tazama! Mimi naona wanaume wanne wakitembea wakiwa huru katikati ya moto,

SURA 3

a Da 2:49

b Da 3:18
Da 3:28

c Met 29:22
Da 2:12

d Da 1:7

e Isa 46:1
Yer 50:2

f Da 3:28

g Da 3:10

h Kut 5:2
2Nya 32:15
Isa 36:20
Isa 37:23

i Lu 12:11
Lu 21:14
Mdo 5:29

j 1Sa 17:37
2Sa 22:26
Zb 27:1
Met 18:10
Isa 12:2
Da 6:27
Mik 7:7
2Ko 1:10

Safu ya 2

a Kut 20:5
Law 19:4
Met 28:1
Mdo 5:29
Ebr 11:34

b 2Sa 22:40
Yer 48:14

c Da 3:15

d Zb 34:19

e Zb 66:12
Zb 91:1
Isa 43:2

nao hawana dhara lolote, na
sura ya yule wa nne inafanana
na mwana wa miungu."[a]
26 Ndipo Nebukadneza aka-
karibia mlango wa tanuru ina-
yowaka moto.[b] Akajibu na ku-
sema: "Shadraki, Meshaki na
Abednego, enyi watumishi wa
Mungu Aliye Juu Zaidi,[c] toke-
ni nje, mje hapa!" Ndipo Sha-
draki, Meshaki na Abedne-
go wakaanza kutoka katikati
ya moto ule. **27** Na maliwa-
li, manaibu wa maliwali, ma-
gavana na maofisa wakuu[d] wa
mfalme waliokuwa wameku-
sanyika wakawaona hao wa-
naume, kwamba ule moto ha-
ukuwa na nguvu juu ya miii-
li yao,[e] wala unywele wowote
wa vichwa vyao haukuwa ume-
ungua,[f] wala hata nguo zao za
kujitanda hazikuwa zimebadi-
lishwa, wala harufu ya moto
haikuwapata.
28 Nebukadneza akajibu na
kusema: "Abarikiwe Mungu wa
Shadraki, Meshaki na Abedne-
go,[g] aliyemtuma malaika wake[h]
na kuwaokoa watumishi wake
waliomtegemea,[i] na ambao wali-
badili neno la mfalme na kutoa
miili yao, kwa maana hawaku-
tumikia kamwe[j] wala kuabudu[k]
mungu yeyote mwingine ila Mu-
ngu wao wenyewe.[l] **29** Nami
natoa agizo,[m] kwamba kikundi
chochote cha watu, cha taifa au
lugha ambacho kinasema jambo
lolote baya juu ya Mungu wa
Shadraki, Meshaki na Abedne-
go, kikatwe vipande-vipande,[n]
na nyumba zao zigeuzwe kuwa
choo cha watu wote;[o] kwa maa-
na hakuna mungu mwingine ye-
yote anayeweza kuokoa kama
huyu."[p]

SURA 3

a Ayu 38:7
Zb 34:7
b Da 6:20
c Mwa 14:18
Da 2:47
1Ko 8:5
d Da 3:2
e Isa 43:2
Ebr 11:34
f Mt 10:30
Lu 21:18
Mdo 27:34
g Da 2:47
Da 4:34
h Zb 34:7
Ebr 1:14
i 1Nya 5:20
Zb 3:8
Zb 22:4
Zb 91:14
2Ko 1:9
Ebr 11:6
j Kut 23:24
Ufu 12:11
k Da 3:5
Da 3:15
l Kut 20:5
Mt 4:10
m Da 6:26
n Da 2:5
o Ezr 6:11
p Kum 32:31
Da 4:35
Da 6:27

Safu ya 2

a Zb 1:3
Da 2:49
Da 3:12

SURA 4

b Est 8:9
Da 3:4
c Da 6:25
d Zb 66:16
Da 2:23
e Kum 4:34
Zb 71:19
Da 6:27
Ro 11:33
f Zb 10:16
Zb 29:10
Zb 66:7
Zb 90:2
Yer 10:10
g Zb 146:10
h Isa 47:8
i Lu 11:21
j Da 5:6
k Da 2:1
l Mwa 41:8
Da 2:2
m Da 5:7
n Isa 47:13
Da 2:27
o Da 2:11
p Da 1:7
Da 5:12
q Isa 46:1
Yer 50:2

30 Ndipo mfalme akawafa-
nya Shadraki, Meshaki na
Abednego wafanikiwe katika
wilaya ya utawala ya Babiloni.[a]

4 "Mfalme Nebukadneza,
kwa vikundi vyote vya
watu, vya mataifa na lugha
ambavyo vinakaa katika du-
nia yote:[b] Amani yenu na iwe
nyingi.[c] **2** Nimeona vema ni-
tangaze ishara na maajabu
ambayo Mungu Aliye Juu Zaidi
amenifanyia.[d] **3** Jinsi zilivyo
kuu ishara zake, na jinsi ma-
ajabu yake yalivyo yenye ngu-
vu![e] Ufalme wake ni ufalme wa
mpaka wakati usio na kipimo,[f]
na utawala wake ni wa kizazi
baada ya kizazi.[g]
4 "Mimi, Nebukadneza, nili-
kuwa nikistarehe[h] nyumba-
ni mwangu, na kufanikiwa ka-
tika jumba langu la kifalme.[i]
5 Kuna ndoto ambayo nilio-
na, nayo ikaanza kuniogope-
sha.[j] Na kulikuwa na picha
za mawazo kitandani mwa-
ngu na maono ya kichwa
changu yaliyoanza kuniogo-
pesha.[k] **6** Nami nikatoa agi-
zo kwamba watu wote wenye
hekima wa Babiloni waletwe
mbele yangu, ili wanijulishe ta-
fsiri ya ndoto hiyo.[l]
7 "Ndipo makuhani wenye
kufanya uchawi, wafanya-ma-
zingaombwe, Wakaldayo[m] na
wanajimu[n] walikuwa wana-
ingia; nami nikasema mbele
yao ndoto ile ilikuwa nini, bali
tafsiri yake hawakuniambia.[o]
8 Mwishowe Danieli akai-
ngia mbele yangu, ambaye jina
lake ni Belteshaza[p] kulingana
na jina la mungu wangu[q] na
ambaye ndani yake mna roho

ya miungu mitakatifu;[a] nami
nikasema mbele yake ndoto ile:
9 "'Ee Belteshaza mkuu wa
makuhani wenye kufanya uchawi,[b] kwa kuwa mimi mwenyewe najua vema kwamba roho
ya miungu mitakatifu imo ndani yako[c] na kwamba hakuna siri
yoyote ambayo inakusumbua,[d]
niambie maono ya ndoto yangu ambayo nimeona na tafsiri yake.[e]
10 "'Basi katika maono ya kichwa changu kitandani mwangu nikawa ninaona,[f] na, tazama! mti[g] fulani katikati ya
dunia, ambao ulikuwa mrefu
sana.[h] **11** Mti huo ulikua, ukawa na nguvu, mwishowe urefu
wake ukafika mbinguni, nao ulikuwa unaonekana mpaka sehemu za mwisho za dunia nzima.[i]
12 Majani yake yalikuwa mazuri, na matunda yake yalikuwa mengi, na juu yake kulikuwa na chakula kwa ajili ya wote.
Chini yake wanyama[j] wa mwituni walitafuta kivuli,[k] na juu
ya matawi yake ndege wa mbinguni walikuwa wakikaa,[l] na
kila kitu chenye mwili kilikuwa kikila chakula kutokana na mti
huo.
13 "'Niliendelea kutazama katika maono ya kichwa changu kitandani mwangu, na, tazama! mlinzi,[m] aliye mtakatifu,[n] akishuka kutoka mbinguni. **14** Alikuwa akiita kwa
sauti kubwa, naye alikuwa akisema hivi: "Ukateni mti uanguke,[o] na kuyakata matawi yake.
Angusheni majani yake, na kutawanya matunda yake. Mnyama na akimbie kutoka chini
yake, na ndege kutoka katika matawi yake.[p] **15** Hata hi-

SURA 4

a Hes 11:17
Isa 63:11
Da 4:18
Da 4:24
Da 5:11
b Da 1:20
Da 2:48
c Mwa 41:38
Da 6:3
d Da 1:17
e Da 2:30
f Da 2:19
g Da 4:26
h Isa 10:33
Eze 31:3
i Mwa 11:4
Mt 11:23
j Yer 27:6
Eze 31:6
k Omb 4:20
l Mt 13:32
m Zb 103:20
Zb 103:21
Da 4:23
n Kum 33:2
Zb 89:7
Da 8:13
Mt 18:10
Lu 4:34
o Eze 21:26
Eze 21:27
Da 4:31
Da 5:20
Lu 3:9
p Yer 51:6
Eze 31:12

Safu ya 2

a Ayu 14:7
Da 4:33
b Da 4:32
c Da 7:25
Da 12:7
Lu 21:24
Ufu 12:14
d Da 4:13
e Zb 83:18
Yer 16:21
Da 4:34
f Zb 75:7
Zb 89:36
Mt 25:31
Lu 1:32
Lu 1:33
g 1Sa 2:8
Eze 17:24
Zek 9:9
Mt 11:29
h Isa 47:13
Da 5:8
Da 5:15
i Mwa 41:16
Da 2:28
Da 4:8
j Da 1:7
k Da 7:28
l 1Sa 3:17
m 2Sa 18:32

vyo, kiacheni kisiki chake katika udongo, kikiwa na pingu
ya chuma na ya shaba, katikati ya majani ya mwituni; na acheni kilowane maji ya umande wa
mbinguni, fungu lake na liwe pamoja na mnyama katikati
ya majani ya nchi.[a] **16** Moyo wake na ubadilishwe usiwe
wa mwanadamu, nao upewe moyo wa mnyama,[b] na nyakati
saba[c] zipite juu yake. **17** Jambo hilo ni kulingana na agizo la walinzi,[d] na ombi hilo ni
kulingana na neno la watakatifu, kusudi watu wanaoishi wa-
jue kwamba Aliye Juu Zaidi ni Mtawala katika ufalme wa wa-
nadamu[e] na kwamba humpa yeyote yule amtakaye ufalme
huo,[f] na humweka juu yake mwanadamu aliye wa hali ya
chini zaidi."[g]
18 "'Hiyo ndiyo ndoto ambayo mimi, Mfalme Nebukadneza, niliona; nawe, Ee Belteshaza, sema tafsiri yake, kwa maana watu wengine wote wenye
hekima wa ufalme wangu wameshindwa kunijulisha tafsiri yake.[h] Bali wewe una uwezo,
kwa kuwa roho ya miungu mitakatifu imo ndani yako.'[i]
19 "Ndipo Danieli, ambaye jina lake ni Belteshaza,[j] alishangaa kwa muda fulani, na
mawazo yake yakaanza kumwogopesha.[k]
"Mfalme akasema, 'Ee Belteshaza, usiache ndoto ile na tafsiri yake ikuogopeshe.'[l]
"Belteshaza akajibu na kusema, 'Ee bwana wangu, ndoto
hiyo na iwahusu wale wanaokuchukia, na tafsiri yake iwahusu adui zako.[m]
20 "'Mti ulioona, ambao ulikua, ukawa mkubwa na ku-

pata nguvu, na ambao urefu
wake mwishowe ulifika mbi-
nguni na ambao ulionekana
duniani kote,[a] **21** na maja-
ni yake yalikuwa mazuri, na
ambao matunda yake yaliku-
wa mengi, na ambao juu yake
kulikuwa na chakula kwa ajili
ya wote; ambao chini yake wa-
nyama wa mwituni walikaa, na
ambao juu ya matawi yake nde-
ge wa mbinguni walikuwa wa-
kikaa,[b] **22** ni wewe, Ee mfa-
lme,[c] kwa sababu wewe ume-
kuwa mkubwa ukapata nguvu,
na ukuu wako umekuwa mku-
bwa na kufika mbinguni,[d] na
utawala wako umefika mpaka
sehemu za mwisho za dunia.[e]

23 "'Na kwa sababu mfalme
aliona mlinzi, aliye mtakati-
fu,[f] akishuka kutoka mbingu-
ni, ambaye pia alikuwa akise-
ma: "Ukateni mti uanguke, na
kuuharibu. Hata hivyo, kia-
cheni kisiki chake katika udo-
ngo, lakini kikiwa na pingu ya
chuma na ya shaba, katikati ya
majani ya mwituni, na kilowa-
ne maji kwa umande wa mbi-
nguni, fungu lake na liwe pa-
moja na wanyama wa mwitu-
ni mpaka nyakati saba zipite
juu yake,"[g] **24** hii ndiyo ta-
fsiri, Ee mfalme, na amri[h] ya
Aliye Juu Zaidi[i] ndiyo itakayo-
mpata bwana wangu mfalme.[j]
25 Nawe watakufukuzia mba-
li kutoka kati ya wanadamu,
na makao yako yatakuwa pa-
moja na wanyama wa mwitu-
ni,[k] nao watakupa majani ule
kama ng'ombe,[l] nawe utalowa-
na maji kwa umande wa mbi-
nguni, na nyakati saba[m] zita-
pita juu yako, mpaka ujue ya
kuwa Aliye Juu Zaidi ni Mta-
wala katika ufalme wa wana-
damu,[a] na kwamba humpa ye-
yote yule amtakaye ufalme
huo.[b]

26 "'Na kwa kuwa walisema
kisiki cha mti huo kiachwe,[c]
ufalme wako utakuwa hakika
kwako baada ya wewe kujua
kwamba mbingu zinatawala.[d]
27 Kwa hiyo, Ee mfalme, sha-
uri langu na likubalike kwako,[e]
nawe uziondoe dhambi zako
kwa uadilifu,[f] na uovu wako
kwa kuwaonyesha maskini re-
hema.[g] Labda mafanikio yako
yatarefushwa.'"[h]

28 Hayo yote yalimpata Mfa-
lme Nebukadneza.[i]

29 Mwishoni mwa miezi
kumi na miwili, alikuwa akite-
mbea juu ya jumba la mfalme
la Babiloni. **30** Mfalme aliku-
wa anasema:[j] "Je, hili si Babilo-
ni Mkubwa, ambalo mimi mwe-
nyewe nimelijenga kwa ajili ya
nyumba ya kifalme kwa nguvu
za uwezo wangu[k] na kwa ajili
ya heshima ya utukufu wa enzi
yangu?"[l]

31 Neno lile lilipokuwa bado
kinywani mwa mfalme, sau-
ti ikashuka kutoka mbinguni:
"Wewe unaambiwa, Ee Mfalme
Nebukadneza, 'Ufalme ume-
ondoka kwako.[m] **32** Nao wa-
nakufukuzia mbali kutoka kati
ya wanadamu, na makao yako
yatakuwa pamoja na wanyama
wa mwituni.[n] Watakupa maja-
ni ule kama ng'ombe, na nya-
kati saba zitapita juu yako,
mpaka ujue kwamba Aliye Juu
Zaidi ni Mtawala katika ufalme
wa wanadamu, na kwamba hu-
mpa yeyote yule amtakaye ufa-
lme huo.'"[o]

SURA 4

a Eze 31:3
Da 4:10
b Da 4:12
c Da 2:37
d Isa 14:13
Isa 14:14
e Da 2:38
f Hes 22:32
Kum 33:2
Zb 89:7
Da 4:13
Da 8:13
Mt 18:10
Mdo 10:3
Mdo 12:23
g Da 4:16
Da 5:21
Lu 21:24
h Isa 23:9
Isa 55:11
Da 4:17
i Zb 83:18
j Ayu 34:19
Zb 107:40
k Da 4:32
Da 5:21
l Zb 106:20
m Da 4:16
Lu 21:24

Safu ya 2

a Zb 83:18
b Ayu 34:24
Yer 27:5
Da 2:21
Da 5:21
Da 7:14
c Da 4:15
d Zb 11:4
Isa 66:1
e Zb 119:46
f Met 16:6
Met 28:13
Isa 55:7
Eze 18:21
Mt 3:8
g Zb 41:1
Isa 58:7
Mik 6:8
1Yo 3:17
h 1Fa 21:29
Yoe 2:14
Yon 3:10
i Hes 23:19
Met 10:24
Isa 55:11
j Zb 73:9
k Met 16:18
l Zb 49:11
m Da 4:25
Mdo 12:23
n Da 4:14
Da 5:21
o Da 4:17

33 Wakati huohuo[a] neno lile likatimia juu ya Nebukadneza, naye akafukuziwa mbali kutoka kati ya wanadamu, akaanza kula majani kama ng'ombe. Mwili wake ukalowana maji kwa umande wa mbinguni, mpaka nywele zake zikawa ndefu kama manyoya ya tai na kucha zake kama kucha za ndege.[b]

34 "Na mwishoni mwa siku zile,[c] mimi, Nebukadneza, niliinua macho yangu juu kuelekea mbinguni,[d] ndipo uelewaji wangu ukaanza kurudi kwangu; nami nikambariki Aliye Juu Zaidi,[e] nami nikamsifu na kumtukuza Yeye anayeishi mpaka wakati usio na kipimo,[f] kwa maana utawala wake ni utawala wa mpaka wakati usio na kipimo na ufalme wake ni wa kizazi baada ya kizazi.[g] **35** Na wakaaji wote wa dunia wanaonwa kuwa si kitu,[h] naye anafanya kulingana na mapenzi yake kati ya majeshi ya mbinguni na wakaaji wa dunia.[i] Wala hakuna yeyote anayeweza kuzuia mkono wake[j] au anayeweza kumuuliza, 'Umekuwa ukifanya nini?'[k]

36 "Ndipo wakati huohuo uelewaji wangu ukaanza kurudi kwangu, nayo heshima ya ufalme wangu, utukufu wangu wa enzi na fahari zikaanza kurudi kwangu;[l] nao maofisa wangu wakuu wa kifalme na wakuu wangu wakaanza kunitafuta kwa hamu, nami nikarudishwa tena juu ya ufalme wangu mwenyewe, nikaongezewa ukuu usio wa kawaida.[m]

37 "Basi mimi, Nebukadneza, namsifu na kumkweza na kumtukuza Mfalme wa mbinguni,[a] kwa sababu kazi zake zote ni kweli na njia zake ni haki,[b] na kwa sababu wale wanaotembea kwa kiburi yeye anaweza kuwafedhehesha."[c]

5 Mfalme Belshaza[d] naye alifanya karamu kwa ajili ya wakuu wake elfu, naye akanywa divai mbele ya hao elfu.[e] **2** Akiwa amechochewa na divai,[f] Belshaza akasema viletwe vyombo vya dhahabu na fedha[g] ambavyo Nebukadneza baba yake alikuwa amevichukua kutoka hekalu lililokuwa Yerusalemu, ili mfalme na wakuu wake, masuria wake na wake zake wadogo wavinywee.[h] **3** Basi wakavileta ndani vile vyombo vya dhahabu ambavyo walikuwa wamevitoa katika hekalu la Mungu lililokuwa Yerusalemu, naye mfalme na wakuu wake, masuria wake na wake zake wadogo wakavinywea. **4** Wakanywa divai, wakaisifu miungu ya dhahabu na fedha, shaba, chuma, miti na mawe.[i]

5 Ndipo wakati huohuo vidole vya mkono wa mtu vikatokea na kuandika mbele ya kinara cha taa juu ya lipu ya ukuta wa jumba la mfalme,[j] naye mfalme akawa anaona sehemu ya nyuma ya mkono uliokuwa ukiandika. **6** Na wakati huo, kwa habari ya mfalme, sura yake ikabadilika, mawazo yake yakaanza kumwogopesha,[k] viungo vya viuno vyake vikalegea,[l] magoti yake yakawa yanagongana.[m]

7 Mfalme akaita kwa sauti kubwa akasema waletwe ndani wafanya-mazingaombwe, Wa-

SURA 4
a Da 3:6 Da 5:5
b Da 4:25
c Da 4:16
d Zb 121:1 Zb 123:1 Zb 123:2
e Zb 7:17 Zb 92:1
f Yer 10:10 1Ti 1:17 Ufu 4:11
g Zb 10:16 Da 4:3 Mik 4:7
h Zb 39:5 Isa 40:15
i 1Sa 3:18 Zb 33:11 Isa 46:10
j Ayu 34:24 Isa 43:13 1Ko 10:22
k Ayu 9:12 Isa 45:9 Ro 9:20
l 2Nya 33:13 Da 4:26
m Met 22:4

Safu ya 2
a Da 4:3 Mdo 17:24
b Kum 32:4 Zb 33:5 Ufu 15:3
c Kut 18:11 Ayu 40:11 Yak 4:6

SURA 5
d Da 5:9 Da 7:1 Da 8:1
e Isa 21:5 Yer 51:39
f Met 20:1 Met 31:4
g 2Fa 25:15 2Nya 36:18 Ezr 1:7 Yer 27:16 Yer 52:19 Da 1:2
h Met 11:2
i Zb 115:4 Zb 135:15 Mdo 17:29 Ufu 9:20
j Da 5:24
k Zb 102:15
l Zb 69:23 Isa 21:3
m Eze 7:17 Nah 2:10

kaldayo na wanajimu.[a] Mfalme
akawaambia watu wenye hekima wa Babiloni: "Mtu yeyote
atakayesoma maandishi haya
na kunionyesha tafsiri yake
kamili, atavikwa mavazi ya
zambarau,[b] pamoja na mkufu
wa dhahabu shingoni mwake,
naye atakuwa mtawala wa tatu
katika ufalme."[c]
8 Basi wakaingia watu wote
wenye hekima wa mfalme, lakini hawakuwa na uwezo wa kutosha kuweza kusoma maandishi hayo wala kumwambia mfalme tafsiri yake.[d] **9** Kwa hiyo
Mfalme Belshaza akaogopa
sana na rangi ya uso wake ikaanza kubadilika ndani yake; na
wakuu wake wakahangaika.[e]
10 Malkia naye, kwa sababu
ya maneno ya mfalme na wakuu wake, akaingia ndani ya jumba la karamu. Malkia akasema: "Ee mfalme, uishi mpaka
wakati usio na kipimo.[f] Usiache mawazo yako yakuogopeshe, wala rangi ya uso wako
ibadilike. **11** Kuna mtu mwenye uwezo katika ufalme wako
ambaye ndani yake mna roho
ya miungu mitakatifu;[g] na katika siku za baba yako nuru na
ufahamu na hekima kama hekima ya miungu zilipatikana ndani yake, na baba yako mwenyewe, Mfalme Nebukadneza, akamweka awe mkuu[h] wa makuhani wenye kufanya uchawi,
na wafanya-mazingaombwe, na
Wakaldayo na wanajimu, Ee
mfalme; **12** kwa kuwa roho
isiyo ya kawaida na ujuzi na ufahamu wa kutafsiri ndoto[i] na kueleza vitendawili na kufungua
mafundo ilikuwa imepatikana
ndani yake,[j] ndani ya Danieli,

SURA 5

a Mwa 41:8
Da 2:2
Da 4:6
b Mwa 41:42
1Sa 17:25
c Da 2:6
Da 2:48
Da 6:2
d Mwa 41:8
Da 2:27
Da 4:7
e Isa 13:7
f Da 3:9
g Da 2:47
Da 4:8
Da 4:18
h Da 2:48
Da 4:9
i Da 1:17
Da 6:3
j 1Fa 4:30
Da 5:16

Safu ya 2

a Da 1:7
Da 4:8
b Da 1:6
Da 2:25
Da 6:13
c 2Fa 24:14
d Da 1:17
Da 2:23
Da 4:9
e Met 2:6
Da 1:20
f Isa 47:12
Da 2:10
Da 5:8
g Mwa 40:8
Da 2:28
h Da 2:6
Da 5:7
i Est 8:15
j Zb 119:46
k Zb 47:2
Zb 83:18
Zb 92:8
Da 4:17
l Da 5:11
m Da 2:37
Da 2:38

ambaye mfalme alimpa jina Belteshaza.[a] Basi Danieli na aitwe, apate kuonyesha tafsiri
kamili."
13 Basi Danieli akaletwa
mbele ya mfalme. Mfalme akasema na kumuuliza Danieli:
"Je, wewe ndiye Danieli ambaye
ni mmoja wa wahamishwa wa
Yuda,[b] ambao baba yangu mfalme aliwatoa Yuda?[c] **14** Nimesikia pia kuhusu wewe kwamba roho ya miungu imo ndani
yako,[d] na nuru na ufahamu na
hekima[e] isiyo ya kawaida zimepatikana ndani yako. **15** Basi
watu wenye hekima na wafanya-mazingaombwe wameletwa mbele yangu, ili wasome
maandishi haya, waniambie tafsiri yake; lakini hawana uwezo
wa kutosha kunionyesha tafsiri
kamili ya neno hilo.[f] **16** Nami
mwenyewe nimesikia habari
zako, kwamba unaweza kutoa
tafsiri[g] na kufungua mafundo.
Basi, ukiweza kusoma maandishi haya na kunijulisha tafsiri
yake kamili, utavikwa mavazi
ya zambarau, pamoja na mkufu wa dhahabu shingoni mwako, nawe utakuwa mtawala wa
tatu katika ufalme."[h]
17 Ndipo Danieli akajibu na
kusema mbele ya mfalme: "Zawadi zako na ziwe zako mwenyewe, na tuzo zako uwape
wengine.[i] Hata hivyo, mimi nitamsomea mfalme maandishi
haya, nami nitamjulisha tafsiri yake.[j] **18** Basi wewe, Ee
mfalme, Mungu Aliye Juu Zaidi[k] alimpa baba yako Nebukadneza[l] ufalme na ukuu na heshima na utukufu wa enzi.[m]
19 Na kwa sababu ya ukuu
ambao Yeye alimpa, vikundi
vyote vya watu, vya mataifa

na lugha vilitetemeka na kuogopa mbele yake.[a] Mtu yeyote aliyetaka kumuua, alimuua; mtu yeyote aliyetaka kumpiga, alimpiga; na mtu yeyote aliyetaka kumwinua, alimwinua; na mtu yeyote aliyetaka kumfedhehesha, alimfedhehesha.[b] **20** Lakini moyo wake ulipojivuna na roho yake ikawa ngumu, akatenda kwa kimbelembele,[c] alishushwa kutoka katika kiti cha ufalme wake, akaondolewa heshima yake.[d] **21** Naye akafukuziwa mbali kutoka kati ya wanadamu, na moyo wake ukafanywa kama ule wa mnyama, naye akakaa pamoja na punda-mwitu.[e] Wakawa wanampa majani ale kama ng'ombe, mwili wake ukalowa maji kwa umande wa mbingu,[f] mpaka alipojua kwamba Mungu Aliye Juu Zaidi ni Mtawala katika ufalme wa wanadamu, na kwamba humweka juu yake yeyote yule anayemtaka.[g]

22 "Na wewe, Belshaza mwana wake,[h] hukunyenyekeza moyo wako,[i] ijapokuwa ulijua hayo yote.[j] **23** Bali ulijiinua juu ya Bwana wa mbingu,[k] nao wakaleta mbele yako vyombo vya nyumba yake;[l] na wewe pamoja na wakuu wako, masuria wako na wake zako wadogo mmekuwa mkivinywea divai. Nawe umeisifu miungu minyonge ya fedha na ya dhahabu, shaba, chuma, miti na mawe,[m] ambayo haioni chochote, wala kusikia chochote, wala kujua chochote;[n] lakini hukumtukuza[o] Mungu ambaye pumzi yako imo mkononi mwake[p] na ambaye njia zako zote ni zake.[a] **24** Basi sehemu ya nyuma ya mkono ilitumwa kutoka mbele zake, na maandishi haya yakaandikwa.[b] **25** Na haya ndiyo maandishi ambayo yaliandikwa: MENE, MENE, TEKELI na PARSINI.

26 "Hii ndiyo tafsiri ya neno: MENE, Mungu amehesabu siku za ufalme wako naye ameukomesha.[c]

27 "TEKELI, wewe umepimwa katika mizani, ukaonekana kuwa umepungukiwa.[d]

28 "PERESI, ufalme wako umegawanywa na kupewa Wamedi na Waajemi."[e]

29 Ndipo Belshaza akatoa amri, nao wakamvika Danieli mavazi ya zambarau, pamoja na mkufu wa dhahabu shingoni mwake; nao wakatangaza kumhusu yeye kwamba atakuwa mtawala wa tatu katika ufalme.[f]

30 Usiku huohuo Belshaza mfalme Mkaldayo akauawa,[g] **31** naye Dario[h] Mmedi akaupokea ufalme, akiwa na umri wa kama miaka 62.

6 Ilionekana vema kwa Dario, naye akaweka maliwali 120 juu ya ufalme, ili wawe juu ya ufalme wote;[i] **2** na juu yao maofisa wakuu watatu, ambao Danieli alikuwa mmoja wao,[j] ili maliwali[k] hao wawe wakiwapa habari sikuzote ili mfalme asipate hasara.[l] **3** Basi ikawa kwamba Danieli huyo akajipatia sifa[m] juu ya wale maofisa wakuu na maliwali, kwa maana roho isiyo ya kawaida ilikuwa ndani yake;[n]

SURA 5
a Yer 25:9; Da 3:4; Da 4:22
b Met 16:14; Da 2:12; Da 3:6; Da 3:29
c Met 16:5; Isa 14:13; Da 4:30; Mik 6:8
d Isa 47:1
e Da 4:25; Da 4:32
f Da 4:33
g Ayu 34:24; Zb 83:18; Eze 17:24; Da 4:17; Da 4:35
h Da 5:11; Da 5:18
i Mt 23:12
j Lu 12:47; Yak 4:17
k Isa 37:23; Yer 50:29
l Da 5:3
m Isa 37:19; Mdo 17:29
n Kum 32:21; Zb 115:5; Zb 135:17; Isa 46:7; 1Ko 8:4
o Ro 1:21
p Zb 104:29; Isa 42:5; Mdo 17:25

Safu ya 2
a Met 20:24; Yer 10:23
b Da 5:5
c Isa 13:11; Yer 25:12; Yer 27:7; Yer 50:1; Yer 51:11
d Ayu 31:6; Ro 2:6; 1Ko 3:13; Kol 3:25
e Ezr 1:1; Isa 21:2; Isa 45:1; Yer 50:9; Da 6:28; Da 9:1
f Isa 14:2; Da 5:7; Da 5:16
g Isa 21:9; Yer 51:8; Yer 51:31; Yer 51:39; Yer 51:57
h Da 6:1; Da 9:1

SURA 6
i Est 1:1
j Met 3:16; Isa 14:2; Da 2:48; Da 5:29
k Ezr 8:36; Est 8:9; Da 3:2
l Ezr 4:22; Est 7:4; Lu 19:23

m Met 3:35; Met 22:29; n Da 1:17; Da 5:12.

naye mfalme alikuwa anakusudia kumwinua juu ya ufalme wote.

4 Ndipo maofisa wakuu na maliwali walikuwa wanatafuta daima kisingizio fulani juu ya Danieli kuhusiana na ufalme huo;[a] lakini hawakuweza kupata kisingizio chochote wala jambo lolote lenye ufisadi, kwa vile alikuwa mwenye kutegemeka wala haukupatikana ndani yake uzembe wowote wala jambo lolote lenye ufisadi.[b] **5** Basi wanaume hao wakasema: "Hatutapata kisingizio chochote juu ya Danieli huyu, isipokuwa tukitafute juu yake katika sheria ya Mungu wake."[c]

6 Basi hao maofisa wakuu na maliwali wakaingia kwa mfalme pamoja,[d] nao wakamwambia jambo hili: "Ee Mfalme Dario, uishi mpaka wakati usio na kipimo.[e] **7** Maofisa wote wakuu wa ufalme, manaibu wa maliwali na maliwali, maofisa wakuu wa kifalme na magavana, wamefanya shauri pamoja ili kuweka sheria ya kifalme[f] na kupiga marufuku, kwamba mtu yeyote atakayetoa ombi kwa mungu yeyote au mwanadamu kwa siku 30 isipokuwa kwako, Ee mfalme, atupwe ndani ya shimo la simba.[g] **8** Na sasa, Ee mfalme, isimamishe imara sheria hiyo na kutia sahihi maandishi hayo,[h] ili yasibadilishwe, kulingana na sheria ya Wamedi na Waajemi,[i] ambayo haifutwi."[j]

9 Kulingana na hayo, Mfalme Dario akatia sahihi maandishi hayo na ile amri ya marufuku.[k]

SURA 6

a Zb 37:12
Met 29:27
Mhu 4:4

b Flp 2:15
1Pe 2:12

c Est 3:8

d Zb 56:6
Met 6:18

e Ne 2:3
Da 2:4

f Zb 59:3
Zb 94:20

g Da 3:6
Da 6:16
Da 6:24

h Est 3:12
Est 8:10

i Est 1:19

j Est 8:8

k Da 6:7

Safu ya 2

a 1Fa 8:30
1Fa 8:44
2Nya 6:38
Zb 5:7

b 1Fa 8:54
2Nya 6:13
Ezr 9:5
Zb 95:6
Lu 22:41
Mdo 7:60

c Zb 55:17
Zb 86:3
Kol 4:2

d Zb 34:1
Ro 12:12

e 1Th 5:17

f Zb 10:9
Zb 37:32

g Da 6:7
Da 6:24

h Est 8:8
Da 6:8

i Da 1:6

j Da 2:25
Da 5:13

k Est 3:8

l Mk 6:26

m 1Fa 8:50

10 Lakini mara Danieli alipojua kwamba maandishi hayo yametiwa sahihi, akaingia nyumbani mwake, kisha, huku madirisha yaliyo katika chumba chake cha dari yakiwa yamefunguliwa kwa ajili yake kuelekea Yerusalemu,[a] alikuwa akipiga magoti na kusali[b] mara tatu kwa siku[c] na kutoa sifa mbele za Mungu wake,[d] kama vile alivyokuwa akifanya kwa ukawaida kabla ya hayo.[e] **11** Ndipo hao wanaume wakajazana ndani na kumkuta Danieli akiomba kibali mbele za Mungu wake.[f]

12 Kisha wakakaribia na kusema mbele ya mfalme kuhusu ile amri ya marufuku ya mfalme: "Je, hakuna amri ya marufuku ambayo wewe umetia sahihi inayosema kwamba mtu yeyote anayetoa ombi kwa mungu yeyote au mwanadamu kwa siku 30 isipokuwa kwako, Ee mfalme, atupwe ndani ya shimo la simba?"[g] Mfalme akajibu na kusema: "Jambo hilo limesimamishwa imara kulingana na sheria ya Wamedi na Waajemi, ambayo haifutwi."[h] **13** Papo hapo wakajibu, nao wakasema mbele ya mfalme: "Danieli,[i] ambaye ni mmoja wa wahamishwa wa Yuda,[j] hakukujali wewe, Ee mfalme, wala hakujali ile amri ya marufuku uliyotia sahihi, bali yeye anatoa maombi yake mara tatu kwa siku."[k] **14** Basi mara tu mfalme aliposikia lile neno, likamchukiza sana,[l] naye akaelekeza akili zake kwa Danieli ili amwokoe;[m] naye akazidi kujitahidi kumkomboa mpaka

jua lilipotua. **15** Mwishowe wanaume hao wakaingia pamoja kwa mfalme, nao wakamwambia mfalme: "Ujue, Ee mfalme, ya kuwa sheria ya Wamedi na Waajemi ni kwamba amri ya marufuku[a] au sheria yoyote ambayo mfalme mwenyewe huisimamisha imara haipasi kubadilishwa."[b]

16 Ndipo mfalme akatoa amri, nao wakamleta Danieli na kumtupa ndani ya shimo la simba.[c] Mfalme akamwambia Danieli: "Mungu wako, ambaye unamtumikia daima, yeye mwenyewe atakuokoa."[d] **17** Na jiwe likaletwa na kuwekwa kwenye kinywa cha shimo lile, naye mfalme akalitia muhuri kwa pete yake ya muhuri na kwa pete ya muhuri ya wakuu wake, ili kwamba jambo lolote lisibadilishwe kumhusu Danieli.[e]

18 Ndipo mfalme akaenda katika jumba lake, akafunga usiku kucha,[f] wala hakuna vyombo vyovyote vya muziki vilivyoletwa mbele yake, na usingizi wake ukamtoka.[g] **19** Mwishowe mfalme akaondoka wakati wa mapambazuko, katika nuru ya asubuhi, akafanya haraka kwenda moja kwa moja kwenye lile shimo la simba. **20** Alipolikaribia lile shimo, akampaazia Danieli sauti kwa huzuni. Mfalme akasema kwa sauti na kumwambia Danieli: "Ee Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, je, Mungu wako unayemtumikia daima[h] amekuokoa kutoka kwa hao simba?"[i] **21** Mara moja Danieli akasema na mfalme: "Ee mfalme, uishi mpaka wakati usio na kipimo. **22** Mungu wangu mwenyewe[a] alimtuma malaika[b] wake na kufunga vinywa vya simba,[c] nao hawakuniangamiza, kwa kuwa nimeonekana kuwa mtu asiye na hatia mbele zake;[d] na pia mbele yako, Ee mfalme, mimi sijafanya tendo lolote lenye kudhuru."[e]

nitakuchumbia uwe wangu ka-
tika uadilifu na katika haki na
katika fadhili zenye upendo na
katika rehema.[h] **20** Nami ni-
takuchumbia uwe wangu kati-
ka uaminifu; nawe hakika uta-
mjua Yehova.'[i]

21 "'Na itakuwa katika siku
hiyo kwamba mimi nitajibu,'
asema Yehova, 'nitazijibu mbi-
ngu, mbingu nazo zitaijibu du-
nia;[j] **22** dunia nayo itaijibu
nafaka[k] na divai tamu na ma-
futa; vitu hivyo navyo vitaji-
bu Yezreeli ['Mungu atapanda
mbegu'].[l] **23** Nami hakika ni-
tampanda yeye duniani kama
mbegu kwa ajili yangu,[m] nami
nitamwonyesha rehema yeye
ambaye hakuonyeshwa rehe-
ma,[n] nami nitawaambia wale
ambao si watu wangu: "Ninyi
ni watu wangu";[o] wao nao wa-
tasema: "Wewe ni Mungu wa-
ngu."'"[p]

3 Na Yehova akaendelea ku-
niambia: "Nenda tena, mpe-
nde mwanamke anayependwa
na rafiki[q] yako na ambaye

SURA 2
a Isa 17:11; Eze 16:27
b Eze 23:26; Sef 1:13
c Yer 13:26; Eze 16:37; Eze 23:29
d Zb 50:22; Ho 5:14
e Isa 24:8; Yer 7:34; Amo 8:10
f 1Fa 12:32; Amo 5:21
g Isa 1:13
h Zb 80:12; Isa 5:5
i Yer 5:17; Yer 8:13
j Isa 29:17; Yer 26:18; Mik 3:12
k Yer 23:2; Amo 3:2; Zek 10:3
l Amu 3:7; 1Fa 16:31; 2Fa 10:28
m Yer 7:9; Yer 18:15; Ho 11:2
n Eze 23:40
o Yer 2:25
p Isa 17:10; Yer 2:32; Eze 22:12
q Eze 20:35
r Isa 40:2
s Kum 30:5; Isa 65:21; Yer 32:15; Eze 28:26; Amo 9:14
t Yos 7:26; Isa 65:10
u Yer 2:2; Eze 16:22
v Kut 15:1; Ho 12:13

Safu ya 2
a Isa 54:5; Yer 3:14
b Kut 23:13; Yos 23:7; Zek 13:2
c Yer 10:11
d Isa 11:6; Eze 34:25
e Zb 46:9; Isa 2:4; Eze 39:9; Zek 9:10
f Law 26:5; Yer 23:6; Eze 34:25; Mik 4:4
g Yer 3:14
h Zb 85:10; Yer 4:2; Mik 7:18
i Isa 54:13; Yer 9:24; Yer 24:7; Yer 31:34; Eze 38:23; Ebr 8:11
j Kum 28:12; Zek 8:12
k Zb 72:16
l Ho 1:11
m Yer 31:27; Zek 10:9
n Ro 11:30
o Ro 9:25; 1Pe 2:10
p Ho 1:10; Zek 13:9; **SURA 3** q Yer 3:20; Ho 1:3.

anafanya uzinzi, kama vile Yehova alivyowapenda wana wa Israeli[a] ingawa wanageukia miungu mingine[b] na kupenda keki za zabibu kavu."[c]

2 Nami nikajinunulia huyo mwanamke kwa vipande kumi na tano vya fedha[d] na kipimo kimoja cha homeri ya shayiri na nusu homeri ya shayiri. **3** Ndipo nikamwambia: "Utakaa ukiwa wangu muda wa siku nyingi.[e] Usifanye uasherati,[f] nawe usiwe wa mwanamume mwingine;[g] nami pia nitakuwa vivyo hivyo kwako."

4 Hiyo ni kwa sababu wana wa Israeli watakaa muda wa siku nyingi bila mfalme[h] wala mkuu wala dhabihu[i] wala nguzo wala efodi[j] wala terafimu.[k] **5** Baadaye wana wa Israeli watarudi na hakika watamtafuta Yehova Mungu wao,[l] na Daudi mfalme wao;[m] nao watakuja kwa Yehova[n] na kwa wema wake wakitetemeka katika siku za mwisho.[o]

4 Sikieni neno la Yehova, enyi wana wa Israeli, kwa maana Yehova ana kesi na wakaaji wa nchi,[p] kwa maana hakuna kweli[q] wala fadhili zenye upendo wala kumjua Mungu katika nchi.[r] **2** Kuna mambo ambayo yameenea, kutangaza laana[s] na kuzoea kufanya udanganyifu[t] na uuaji[u] na wizi[v] na uzinzi,[w] na vitendo vya kumwaga damu vimegusana na vitendo vingine vya kumwaga damu.[x] **3** Ndiyo sababu nchi itaomboleza[y] na kila mkaaji ndani yake atadhoofika pamoja na mnyama wa mwituni na kiumbe kinachoruka cha mbinguni, na hata samaki wa baharini watakusanywa katika kifo.[a]

4 "Hata hivyo, mtu yeyote asishindane,[b] wala mtu yeyote asikaripie, kwa maana watu wako ni kama wale wanaoshindana na kuhani.[c] **5** Nawe hakika utajikwaa wakati wa mchana,[d] na hata nabii atajikwaa pamoja nawe, kama wakati wa usiku.[e] Nami nitamnyamazisha mama yako.[f] **6** Hakika watu wangu watanyamazishwa, kwa sababu hakuna ujuzi.[g] Kwa kuwa wewe mwenyewe umeukataa ujuzi,[h] mimi pia nitakukataa wewe usiwe kuhani kwangu;[i] na kwa sababu unaendelea kuisahau sheria ya Mungu wako,[j] hata mimi nitawasahau wana wako.[k] **7** Kulingana na wingi wao, ndivyo wamenitendea dhambi.[l] Wamebadili utukufu wangu kuwa aibu tupu.[m] **8** Wanazidi kula dhambi ya watu wangu, nao huendelea kuinua nafsi zao kwenye kosa lao.[n]

9 "Na itakuwa kwa watu kama vile itakavyokuwa kwa kuhani;[o] nami hakika nitawatoza hesabu kwa sababu ya njia zao;[p] nami nitarudisha matendo yao juu yao.[q] **10** Nao watakula, lakini hawatashiba.[r] Watawatendea wanawake kama makahaba; lakini hawataongezeka,[s] kwa sababu wameacha kumjali Yehova.[t] **11** Uasherati na divai na divai tamu ndivyo vinavyoondoa kusudi jema.[u] **12** Watu wangu mwenyewe wanaendelea kuuli-

SURA 3
a Kum 7:7; Amu 10:16; 2Fa 13:23; Zb 106:45
b Amu 10:13; Ne 9:18
c Yer 7:18
d Mwa 34:12
e Kum 21:13
f Kum 5:18
g Ro 7:3
h 2Fa 17:6; 2Fa 18:10
i Da 9:27
j Amu 8:27
k Amu 17:5; 1Sa 19:16; Eze 21:21
l Yer 3:22; Yer 50:4
m Yer 30:9; Eze 34:23; Eze 37:22; Amo 9:11; Lu 1:32; Ufu 22:16
n Zb 130:4; Yer 33:9
o Kum 4:30; Mik 4:1

SURA 4
p Isa 3:13; Yer 25:31; Mik 6:2
q Isa 59:13; Yer 6:13; Mik 7:2
r Yer 4:22; Ro 1:28
s Zb 10:7; Zb 59:12
t Zb 5:6; Isa 59:13; Ho 11:12
u 1Fa 21:19; Yer 7:9
v Zek 5:3
w Yer 29:23; Eze 23:37
x Omb 4:13; Ho 6:9; Mt 23:35; Mdo 7:52
y Isa 24:4; Yer 4:28; Yoe 1:10; Amo 8:8

Safu ya 2
a Yer 4:25; Yer 9:10; Yer 12:4; Sef 1:3
b Amo 5:13
c Kum 17:12; Yer 18:18
d Yer 6:4
e Yer 14:15
f Isa 50:1
g Isa 5:13; Yer 4:22
h Yer 2:8; Lu 11:52
i Mt 21:43
j 2Fa 17:16
k Ayu 34:11
l Ezr 9:7
m Ro 1:23
n 1Sa 2:29; Isa 56:11; Mik 3:11
o Isa 24:2

p Ho 12:2; Amo 3:2; Ro 14:12; Ebr 4:13; q Zb 62:12; Met 5:22; Yer 17:10; Zek 1:6; r Law 26:26; Mik 6:14; Hag 1:6; s Ho 9:11; t 2Nya 24:18; Zb 125:5; Eze 18:24; u Met 6:32; Met 20:1; Met 23:33; Isa 28:7.

za habari[a] kutoka kwa sana-
mu yao ya mti,[b] na fimbo yao
ya mkononi huwaambia; kwa
maana roho ya uasherati ime-
wafanya watange-tange,[c] nao
kwa uasherati hutoka chini ya
Mungu wao.[d] **13** Wao hutoa
dhabihu juu ya vilele vya mi-
lima,[e] nao hufukiza moshi wa
dhabihu juu ya vilima,[f] chini
ya mti mnene na mlubna na
mti mkubwa, kwa sababu kivu-
li chake ni kizuri.[g] Ndiyo saba-
bu binti zenu hufanya uashera-
ti na binti-wakwe zenu hufanya
uzinzi.

14 "Sitatoza hesabu juu ya
binti zenu kwa sababu wana-
fanya uasherati, wala juu ya
binti-wakwe zenu kwa sababu
wanafanya uzinzi. Kwa maa-
na, kwa habari ya wanaume,
hujiendea zao wenyewe pamo-
ja na makahaba,[h] nao hutoa
dhabihu pamoja na wana-
wake makahaba wa hekalu-
ni;[i] na watu ambao hawaelewi[j]
watakanyagiwa chini. **15** Ija-
pokuwa unafanya uasherati,
Ee Israeli,[k] Yuda asiwe na ha-
tia,[l] nanyi msije Gilgali,[m] wala
msiende Beth-aveni[n] wala ku-
apa 'Kama anavyoishi Yeho-
va!'[o] **16** Kwa maana, kama
vile ng'ombe mkaidi, ndivyo
Israeli amekuwa mkaidi.[p] Je,
ni wakati huu kwamba Yehova
atawachunga kama vile mwa-
na-kondoo dume katika mahali
penye nafasi pana? **17** Efra-
imu ameshikamana na sana-
mu.[q] Mwache![r] **18** Pombe
yao ya ngano ikishamalizika,[s]
hakika wamemtendea mwa-
namke kama kahaba.[t] Hakika
wanaomkinga[u] wamependa
aibu.[v] **19** Upepo umemfuni-
ka mabawa yake.[w] Nao watapa-
twa na aibu kutokana na dha-
bihu zao."[a]

5 "Sikieni hili, enyi makuha-
ni,[b] na mkaze uangalifu,
enyi nyumba ya Israeli, na ni-
nyi, enyi nyumba ya mfalme,[c]
tegeni sikio, kwa maana hu-
kumu hii inawahusu ninyi;
kwa maana mmekuwa mtego[d]
katika Mispa na kama wavu
uliotandazwa juu ya Tabori.[e]
2 Na wale wanaoasi wamehu-
sika sana[f] katika kazi ya kuua,
nami nilikuwa himizo kwao
wote.[g] **3** Mimi binafsi nime-
jua Efraimu,[h] Israeli nayo hai-
kufichwa kutoka kwangu.[i]
Kwa sasa, Ee Efraimu, umewa-
tendea wanawake kama maka-
haba;[j] Israeli imejitia unajisi.[k]
4 Matendo yao hayawaruhusu
kurudi kwa Mungu wao,[l] kwa
sababu kuna roho ya uashera-
ti[m] katikati yao; nao hawaku-
mtambua Yehova.[n] **5** Na ki-
buri cha Israeli kimeshuhudia
mbele ya uso wake;[o] na Israeli
na Efraimu wamekwazwa ka-
tika kosa lao.[p] Yuda pia ame-
jikwaa pamoja nao.[q] **6** Wali-
enda kumtafuta Yehova waki-
wa na makundi yao na mifugo
yao, lakini hawakuweza ku-
mpata.[r] Alikuwa amejiondoa
kwao. **7** Wamemtendea hila[s]
Yehova mwenyewe, kwa maa-
na wamezaa wana wa kigeni.[t]
Sasa, mwezi mmoja utawame-
za pamoja na mafungu yao ya
mashamba.[u]

8 "Pigeni baragumu[v] kati-
ka Gibea,[w] tarumbeta kati-
ka Rama! Pigeni kelele za vita
katika Beth-aveni[x]—nyuma
yako, Ee Benyamini![y] **9** Ee

SURA 4

a Yer 2:27
Hab 2:19
b Isa 44:13
c Yer 3:9
d Eze 16:17
e 1Fa 14:23
Isa 65:7
Yer 3:6
Eze 20:28
f 2Fa 17:11
Eze 6:13
g Isa 1:29
Isa 57:5
Yer 2:20
Eze 20:28
h 1Ko 6:16
i Kum 23:17
j Isa 44:18
Yer 4:22
Da 12:10
Ho 14:9
Ro 3:11
Efe 4:18
k Eze 23:5
l 2Fa 17:18
Yer 3:10
m Ho 9:15
Ho 12:11
Amo 4:4
n Ho 5:8
Ho 10:5
o Isa 48:1
Yer 5:2
Eze 20:39
p Zb 78:8
Zb 81:12
Isa 65:2
Zek 7:11
q Ho 11:2
Ho 13:2
r Mt 15:14
s Isa 1:22
t Ho 4:10
u Zb 47:9
v Mik 3:11
Mik 7:3
w Yer 4:11

Safu ya 2

a Isa 42:17
Yer 2:26

SURA 5

b Ho 4:9
Mal 1:6
c Ho 7:3
d Mik 7:2
Hab 1:15
e Amu 4:6
Yer 46:18
f Isa 29:15
g 2Nya 36:15
h Isa 7:9
i Amo 3:2
j Ho 4:18
k Eze 23:5
l Zb 78:8
m Ho 4:12
Amo 2:7
Zek 13:2
n 1Sa 2:12
Yer 9:6
o Met 30:13
Isa 9:9
Ho 7:10
p Met 11:5
q 2Fa 17:19
Eze 23:31
Amo 2:4
r Met 1:28
Isa 1:15
Yer 11:11
Eze 8:18
Mik 3:4

s Isa 48:8; Yer 3:20; t Mal 2:11; u Zek 11:8; v Yer 4:5; Ho 8:1; Yoe 2:1; w Isa 10:29; x Ho 4:15; Ho 10:5; y Amu 5:14.

Efraimu, utakuwa kitu cha kushangaza katika siku ya kukemewa.[a] Nimejulisha maneno yenye kutegemeka[b] kati ya makabila ya Israeli. **10** Wakuu wa Yuda wamekuwa kama watu wanaosogeza nyuma mpaka.[c] Nitamwaga ghadhabu yangu kama maji juu yao. **11** Efraimu ameonewa, amepondwa kwa haki,[d] kwa maana alikuwa amejiamulia mwenyewe kumfuata adui yake.[e] **12** Nami nilikuwa kama nondo[f] kwa Efraimu na kama kuoza kwa nyumba ya Yuda.

13 "Na Efraimu akaona ugonjwa wake, na Yuda kidonda chake.[g] Ndipo Efraimu akaenda Ashuru[h] na kupeleka ujumbe kwa mfalme mkuu.[i] Lakini huyo hakuweza kuwaponya ninyi,[j] wala kuwaondolea kidonda kwa dawa yoyote.[k] **14** Kwa maana mimi nitakuwa kama mwana-simba kwa Efraimu[l] na kama mwana-simba mwenye manyoya shingoni kwa nyumba ya Yuda. Mimi, mimi mwenyewe nitararua vipande-vipande nami nitaenda na kuchukulia mbali, na hapatakuwa na mkombozi.[m] **15** Nitaenda, nitarudi mahali pangu mpaka watakapoibeba hatia yao;[n] nao hakika watautafuta uso wangu.[o] Watanitafuta,[p] wanapokuwa katika dhiki kali."[q]

6 "Njooni, turudi kwa Yehova,[r] kwa maana yeye mwenyewe amerarua vipande-vipande,[s] lakini atatuponya.[t] Alizidi kupiga, lakini atatufunga kitambaa.[u] **2** Atatufanya hai baada ya siku mbili.[v] Katika siku ya tatu atatuinua, nasi tutaishi mbele zake.[w] **3** Nasi tutajua, tutafanya bidii kumjua Yehova.[a] Kutokea kwake kumefanywa imara[b] kama mapambazuko.[c] Naye atakuja kwetu kama mvua inayonyesha;[d] kama mvua ya masika ambayo huilowesha dunia."[e]

4 "Nitakufanyia nini, Ee Efraimu? Nitakufanyia nini, Ee Yuda,[f] wakati fadhili zenu zenye upendo ni kama mawingu ya asubuhi na kama umande ambao hutoweka mapema? **5** Ndiyo sababu nitawakatakata kwa kutumia manabii;[g] nitawaua kwa maneno ya kinywa changu.[h] Na hukumu juu yako zitakuwa kama nuru inayotokea.[i] **6** Kwa maana mimi ninapendezwa na fadhili zenye upendo,[j] na si dhabihu;[k] ninapendezwa na kumjua Mungu kuliko matoleo mazima ya kuteketezwa.[l] **7** Lakini wao wenyewe, kama mtu wa udongo, wamevunja lile agano.[m] Hapo ndipo wamenitendea kwa hila.[n] **8** Gileadi[o] ni mji wa watu wanaotenda madhara; alama za nyayo zao ni damu.[p] **9** Na kama ilivyo katika kumvizia mtu,[q] ushirika wa makuhani ni vikundi vyenye kupora.[r] Wao hufanya mauaji katika Shekemu[s] kando ya njia, kwa sababu wameendeleza mwenendo mpotovu.[t] **10** Nimeona jambo lenye kuchukiza[u] sana katika nyumba ya Israeli. Humo Efraimu[v] anafanya uasherati. Israeli amejitia unajisi.[w] **11** Zaidi ya hilo, Ee Yuda, mavuno yamewekwa kwa ajili yako, wakati nitakapowarudisha tena watu wangu waliotekwa."[x]

SURA 5

a Isa 28:3
b Ho 9:13; Zek 1:6
c Kum 19:14; Kum 27:17; Ayu 24:2; Met 22:28
d Kum 28:33
e 1Fa 20:1
f Isa 50:9; Isa 51:8
g Yer 30:13
h 2Fa 15:29; 2Fa 16:7; Ho 8:9; Ho 12:1
i Ho 10:6
j 2Nya 28:20
k Yer 30:15
l Zb 50:22; Omb 3:10
m Isa 5:29; Amo 2:14
n Law 26:40
o 2Nya 7:14; Yer 29:12; Ho 11:10
p Kum 30:10; Zb 78:34
q Kum 4:30; 1Sa 13:6

SURA 6

r Isa 55:7; Yer 3:22
s Ho 5:14
t Yer 33:6; Ho 14:4
u Kum 32:39; Yer 30:17
v 2Fa 20:5; Isa 26:19; Eze 37:14; 1Ko 15:4
w Ufu 11:11

Safu ya 2

a Isa 54:13; Yer 24:7
b Mal 4:2
c 2Sa 23:4
d Isa 44:3; Yoe 2:23
e Ayu 29:23; Zb 72:6
f Isa 5:3; Ho 11:8
g 2Nya 21:12; Isa 58:1; Yer 1:10; Eze 3:9
h Yer 23:29
i Sef 3:5
j Mik 6:8; Mik 7:18; Mt 12:7
k Met 21:3; Isa 1:11; Mik 6:6; Mt 9:13
l 1Sa 15:22; 1Yo 2:3
m 2Fa 17:15; Isa 24:5; Ho 8:1; Ebr 8:9
n Isa 48:8
o Ho 12:11
p 1Fa 2:5; Mik 7:2
q Met 1:11
r Eze 22:25
s 1Fa 12:25
t Eze 22:9

u Yer 5:30; Yer 23:14; v 2Fa 17:7; Yer 3:6; w Eze 23:4; Eze 23:11; x Kum 30:3; Yer 29:14; Amo 9:14.

7 "Wakati ninapotaka kuponya Israeli,[a] ndipo kosa
la Efraimu pia hufunuliwa,[b] na mambo mabaya ya Sa-
maria;[c] kwa maana wamezoea kusema uwongo,[d] na mwi-
zi huingia ndani; kikundi cha waporaji hushambulia ghafu-
la upande wa nje.[e] **2** Na hawauambii moyo[f] wao kwamba
mimi nitakumbuka ubaya wao wote.[g] Sasa matendo yao yame-
wazunguka.[h] Yamekuja mbele za uso wangu.[i] **3** Wao humfa-
nya mfalme ashangilie kwa ubaya wao, na wakuu kwa
udanganyifu wao.[j] **4** Wote ni wazinzi,[k] kama tanuru amba-
lo mwokaji amewasha, ambaye huacha kuchochea baada ya
kukanda unga mpaka unapotiwa chachu. **5** Wakuu wame-
kuwa wagonjwa[l] katika siku ya mfalme wetu—kuna ghadha-
bu kwa sababu ya divai.[m] Amenyoosha mkono wake pamoja
na wenye kudharau. **6** Kwa maana wameleta moyo wao ka-
ribu kama kwenye tanuru;[n] unawaka ndani yao.[o] Mwokaji
wao analala usiku wote; kufika asubuhi tanuru lao linawaka
kama kwa moto unaotoa mia-
li.[p] **7** Wao wote hupata moto,
kama tanuru, nao huwateketeza waamuzi wao. Wafalme wao
wote wameanguka;[q] hakuna
yeyote kati yao anayeniita.[r]
8 "Lakini Efraimu naye hu-
changamana binafsi na viku-
ndi vya watu.[s] Efraimu ame-
kuwa keki ya mviringo amba-
yo haikugeuzwa upande mwi-
ngine.[t] **9** Wageni wamekula
nguvu zake,[u] na yeye mwe-
nyewe hakupata kujua hilo.[v]
Pia, mvi zimekuwa nyeupe juu
yake, lakini yeye mwenyewe
hakupata kujua hilo. **10** Na
kiburi cha Israeli kimeshuhu-
dia mbele ya uso wake,[a] nao
hawakurudi kwa Yehova Mu-
ngu wao,[b] wala hawakumtafu-
ta kwa sababu ya hayo yote.[c]
11 Na Efraimu ni kama nji-
wa[d] mjinga, asiye na ufaha-
mu.[e] Wameita Misri;[f] wamee-
nda Ashuru.[g]
12 "Njia yoyote ile wanayo-
iendea, nitatandaza juu yao
wavu wangu.[h] Nitawashusha
chini kama viumbe vinavyo-
ruka vya mbinguni.[i] Nitawa-
tia nidhamu kulingana na ha-
bari iliyopelekwa kwenye
kusanyiko lao.[j] **13** Ole wao,[k]
kwa maana wamenikimbia![l]
Na waporwe, kwa maana wa-
menikosea! Nami mwenyewe
nikachukua hatua ya kuwa-
komboa,[m] bali wao wenyewe
wamesema uwongo juu yangu.[n]
14 Nao hawakuniita mimi kwa
moyo[o] wao niwape msaada, inga-
wa waliendelea kupiga mayo-
we vitandani mwao. Wakaen-
delea kuwa na uzembe[p] kwa
sababu ya nafaka na divai yao
tamu; wakazidi kunigeuka
mimi.[q] **15** Na mimi nilitia ni-
dhamu;[r] niliitia mikono yao
nguvu,[s] lakini waliendelea ku-
nipangia mambo mabaya.[t]
16 Nao wakaanza kurudi, la-
kini hawakurudi kwenye iba-
da ya kweli;[u] walikuwa wame-
kuwa kama upinde uliolegea.[v]
Wakuu wao wataanguka kwa
upanga kwa sababu ya shutu-
ma za ulimi wao.[w] Hiyo itaku-
wa ni dhihaka yao katika nchi
ya Misri."[x]

SURA 7

a Kum 32:39
b Isa 28:1
Mik 6:16
c Eze 16:46
Amo 8:14
Mik 1:5
d Yer 9:3
Mik 7:3
e Ho 6:9
f Kum 32:29
Isa 1:3
Isa 44:19
g Yer 14:10
Amo 8:7
h Zb 9:16
Met 5:22
i Zb 90:8
Met 5:21
j 1Fa 22:6
Yer 5:31
Ro 1:32
k Yer 3:9
Mal 3:5
l Met 20:1
Isa 28:1
m Isa 5:11
Hab 2:15
n 2Sa 13:28
o Met 4:16
p Mik 2:1
q 2Fa 15:10
2Fa 15:14
r Isa 9:13
Eze 22:30
Da 9:13
s Zb 106:35
Eze 23:5
t 1Fa 18:21
Ufu 3:15
u 2Fa 13:3
2Fa 15:19
v Met 23:35

Safu ya 2

a Yer 3:3
Ho 5:5
b Ne 9:35
Isa 9:13
Yer 8:5
Amo 4:6
Zek 1:4
c Zb 14:2
Ro 3:11
d Ho 11:11
e Met 15:32
Isa 1:3
f 2Fa 17:4
Isa 30:2
g 2Fa 15:19
Yer 2:18
Eze 23:5
h Eze 12:13
i Mhu 9:12
j Kum 28:15
2Fa 17:13
Isa 28:26
k Isa 31:1
Eze 16:23
l Yer 2:5
m Isa 41:14
Mik 6:4
n Isa 59:13
o Zb 78:37
Isa 29:13
Yer 3:10
Zek 7:5
p Amu 9:27
Amo 2:8
q Zb 78:57
r Zb 94:12
Ebr 12:6
s 2Fa 13:5
t Met 6:14
Nah 1:9
u Yer 3:10

v Zb 78:57; w Zb 12:4; Zb 73:9; Isa 3:8; x Eze 36:20; Ho 9:3.

8 "Tia baragumu[a] katika kinywa chako! Mtu fulani anakuja kama tai[b] juu ya
nyumba ya Yehova, kwa sababu wamelivunja agano langu,[c]
nao wameikosea sheria yangu.[d]
2 Wao wanazidi kunililia, 'Ee
Mungu wangu, sisi, Israeli, tu-
mekujua.'[e]
3 "Israeli ametupilia mba-
li wema.[f] Adui na amfuatilie.[g]
4 Wao wenyewe wameweka
wafalme,[h] lakini si kwa saba-
bu yangu. Wameweka wakuu,
lakini mimi sikuwa na habari.
Wamejifanyia sanamu[i] kwa fe-
dha yao na dhahabu yao, kusu-
di wakatiliwe mbali.[j] **5** Nda-
ma wako ametupiliwa mbali,[k]
Ee Samaria. Hasira yangu ime-
waka juu yao.[l] Wataendelea
mpaka wakati gani kutoweza
kuwa na hali isiyo na hatia?[m]
6 Kwa maana katika Israeli ki-
metokea hata kitu hiki.[n] Fundi
tu ndiye aliyekifanya,[o] wala si
Mungu; kwa maana ndama wa
Samaria atavunjika vipande-
vipande.[p]
7 "Kwa maana wao huende-
lea kupanda upepo, nao wata-
vuna[q] upepo wa dhoruba. Ha-
kuna chochote chenye nafaka
inayosimama.[r] Hakuna chipu-
kizi lolote linalotoa unga.[s] Chi-
pukizi lolote likiutokeza, wa-
geni wataumeza.[t]
8 "Israeli watamezwa.[u] Sasa
watakuja kuwa kati ya mata-
ifa,[v] kama chombo ambacho
hakipendezi.[w] **9** Kwa maa-
na wao wenyewe wamepanda
kwenda Ashuru,[x] kama punda-
milia aliyejitenga.[y] Kwa ha-
bari ya Efraimu, wamekodi
wapenzi.[z] **10** Pia, ingawa wa-
naendelea kuwakodi kati ya
mataifa,[a] sasa mimi nitawaku-
sanya pamoja; nao watakuwa
katika maumivu makali[a] kwa
kitambo kidogo kwa sababu ya
mzigo wa mfalme na wakuu.
11 "Kwa maana Efraimu
amezidisha madhabahu ili ku-
tenda dhambi.[b] Amekuwa na
madhabahu ili atende dhambi.[c]
12 Ndipo nikamwandikia ma-
mbo mengi ya sheria yangu;[d]
nayo yamehesabiwa kuwa
kama kitu kigeni.[e] **13** Walizi-
di kunitolea dhabihu ya nyama
kuwa dhabihu za zawadi,[f] nao
wakaendelea kula vitu amba-
vyo Yehova hakufurahia.[g] Sasa
atakumbuka kosa lao na kuto-
za hesabu kwa sababu ya dha-
mbi zao.[h] Ndipo wao walipo-
rudi Misri.[i] **14** Naye Israeli
akaanza kumsahau Mtengene-
zaji wake[j] na kujenga mahekalu;[k] naye Yuda akazidisha maji-
ji yenye ngome.[l] Nami nitapele-
ka moto katika majiji yake nao
utateketeza minara ya makao
ya kila mmoja."[m]
9 "Usishangilie, Ee Israeli.[n]
Usitende kwa shangwe
kama vikundi vya watu.[o] Kwa
maana kwa kufanya uashera-
ti umeondoka kando ya Mungu
wako.[p] Umependa zawadi za
kukodiwa juu ya viwanja vyote
vya kupuria nafaka.[q] **2** Uwa-
nja wa kupuria na shinikizo la
divai haviwalishi wao,[r] nayo di-
vai tamu inamkatisha tamaa.[s]
3 Hawataendelea kukaa kati-
ka nchi ya Yehova,[t] naye Efrai-
mu atarudi Misri,[u] nao watakula vitu vilivyo najisi katika
Ashuru.[v] **4** Hawataendelea
kummiminia Yehova divai.[w]

SURA 8
a Yer 4:5; Ho 5:8
b Kum 28:49; Yer 48:40; Hab 1:8
c Yer 31:32; Eze 16:59; Ho 6:7
d 2Fa 17:15; Isa 24:5
e Isa 48:1; Mik 3:11; Tit 1:16
f Zb 36:3; Zb 50:17
g Law 26:36; Omb 4:19
h 1Fa 12:20
i 1Fa 12:28; Ho 13:2
j 1Fa 13:34; Yer 44:8
k Isa 45:20; Ho 10:5
l Kum 32:22; 2Fa 17:18
m Yer 4:14; Yer 13:27
n Zb 106:19
o Zb 135:15; Isa 44:9; Yer 10:3; Hab 2:18
p 2Fa 23:15; 2Fa 23:19; 2Nya 31:1
q Ayu 4:8; Met 22:8; Ga 6:7
r Isa 17:11
s Yer 12:13
t Kum 28:33; 2Fa 15:29
u 2Fa 18:11; Yer 50:17; Yer 51:34
v Law 26:33
w Isa 30:14; Yer 22:28; Yer 48:38
x 2Fa 15:19; Eze 23:5; Ho 5:13; Ho 12:1
y Yer 2:24
z Eze 16:33
a Eze 16:37; Eze 23:9

Safu ya 2
a 2Fa 14:26; 1Nya 5:26
b Isa 10:11; Eze 6:13
c Kum 4:28; Ho 12:11
d Kum 4:6; Zb 119:18; Met 22:20
e 2Fa 17:15; Ne 9:26; Isa 30:9
f Yer 7:21
g 1Sa 15:22; Met 21:27; Isa 1:11; Amo 5:22
h Ho 9:9; Amo 8:7
i Ho 7:16; Ho 9:3
j Kum 32:18; Isa 51:13
k 1Fa 12:31
l 2Nya 26:10

m 2Fa 18:13; 2Nya 36:19; Yer 17:27; Yer 34:7;
SURA 9 n Ho 10:5; Amo 6:13; o Eze 20:32; p Eze 23:5; Ho 4:12; q Ho 2:12; Mik 1:7; r Ho 2:9; s Isa 24:7; Amo 5:11; t Law 20:22; Kum 28:64; Yos 23:15; 1Fa 9:7; u Kum 28:68; Ho 8:13; v 2Fa 17:6; Eze 4:13; w Hes 15:5; Hes 28:14; Yoe 1:13.

Na dhabihu zao hazitampendeza;[a] hizo ni kama mkate wa nyakati za maombolezo[b] kwao; wote wanaoula watajitia unajisi. Kwa maana mkate wao ni kwa ajili ya nafsi zao wenyewe; hautaingia katika nyumba ya Yehova.[c] **5** Ninyi mtafanya nini katika siku ya mkutano na katika siku ya sherehe ya Yehova?[d] **6** Kwa maana, tazama! lazima watakwenda kwa sababu ya uporaji.[e] Misri itawakusanya pamoja;[f] Memfisi[g] nayo itawazika. Upupu nao utachukua vitu vyao vyenye kutamanika vya fedha;[h] miti yenye miiba itakuwa katika mahema yao.[i]

7 "Siku za kukaziwa fikira zitakuja;[j] siku za malipo yanayostahili zitakuja.[k] Watu wa Israeli watajua habari hiyo.[l] Nabii atakuwa mpumbavu,[m] mtu wa neno lililoongozwa na roho atatiwa wazimu kwa sababu ya wingi wa makosa yako,[n] hata uadui kuwa mwingi."

8 Mlinzi[o] wa Efraimu alikuwa pamoja na Mungu wangu.[p] Kuhusu nabii,[q] kuna mtego wa mwindaji wa ndege katika njia zake zote;[r] kuna uadui katika nyumba ya Mungu wake. **9** Wamejiingiza sana katika kuleta uharibifu,[s] kama katika siku za Gibea.[t] Atakumbuka kosa lao;[u] atakazia fikira dhambi zao.

10 "Nilimkuta Israeli kama zabibu nyikani.[v] Niliwaona mababu zenu kama tini ya mapema katika mtini ulio katika majira yake ya kwanza.[w] Wao wenyewe waliingia kwa Baali wa Peori,[x] nao wakajiweka wakfu kwa kitu kile cha aibu, wakawa wenye kuchukiza[a] kama kile kitu walichokipenda.[b] **11** Na kwa habari ya Efraimu, utukufu wao hurukia mbali kama kiumbe kinachoruka,[c] hata kusiwe na kuzaa, wala tumbo lenye mimba wala kuchukua mimba.[d] **12** Kwa maana ingawa wanalea wana wao, mimi pia nitawaondolea watoto wao hata kusiwe na mtu;[e] kwa sababu—ole wao pia nitakapogeuka kutoka kwao![f] **13** Efraimu, ambaye nimemwona kama Tiro akiwa amepandwa katika uwanja wa malisho,[g] ndiyo, Efraimu anakusudiwa kumtolea muuaji watoto wake."[h]

14 Wape, Ee Yehova, kile inachokupasa kuwapa.[i] Wape tumbo lenye kuharibu mimba[j] na maziwa yanayokauka.

15 "Ubaya wao wote ulikuwa katika Gilgali,[k] kwa maana hapo nililazimika kuwachukia.[l] Nitawafukuzia mbali kutoka katika nyumba yangu mwenyewe kwa sababu ya uovu wa matendo yao.[m] Sitaendelea kuwapenda.[n] Wakuu wao wote wanatenda kwa ukaidi.[o] **16** Efraimu atapigwa aanguke.[p] Mzizi wao utakauka.[q] Hawatazaa matunda yoyote.[r] Pia, hata wakizaa, nitaviua vitu vyenye kutamanika vya tumbo lao."[s]

17 Mungu wangu[t] atawakataa, kwa maana hawakumsikiliza,[u] nao watakuwa wakimbizi katikati ya mataifa.[v]

10 "Israeli ni mzabibu unaoharibika.[w] Yeye huendelea kutokeza matunda kwa ajili yake mwenyewe.[x] Naye amezidisha madhabahu zake

SURA 9
a Isa 1:11; Yer 6:20
b Kum 26:14
c Hes 28:2
d Yoe 1:14
e Ho 7:13
f Ho 7:16; Ho 8:13
g Yer 2:16
h Met 24:31; Isa 7:23
i Isa 5:6; Isa 32:13; Isa 34:13
j Isa 10:3; Yer 10:15; Lu 19:44
k Lu 21:22
l Zb 9:16
m Isa 44:25; Yer 6:14
n Eze 14:10
o Yer 6:17; Yer 31:6; Eze 33:7
p 1Fa 17:1; 2Fa 2:14
q 1Fa 18:19; Yer 6:14; Yer 14:13
r Omb 2:14
s Isa 31:6
t Amu 19:22; Amu 20:5; Ho 10:9
u Ho 8:13
v Yer 2:2; Yer 31:2
w Hes 13:23; Isa 28:4; Mik 7:1
x Hes 25:3; Kum 4:3; Zb 106:28

Safu ya 2
a 1Fa 16:31; Yer 11:13
b Isa 66:3; Eze 7:20; Amo 4:5
c Yak 1:11
d Kum 28:18
e Kum 28:32; Kum 32:25; Yer 15:7
f Kum 31:17; 2Fa 17:18
g Eze 28:12
h 2Fa 15:16; Yer 9:21
i Lu 23:29
j Zb 58:8
k Ho 4:15; Ho 12:11; Amo 5:5
l Eze 23:18
m Law 26:33; 2Fa 17:18; Zb 78:60; Amo 5:27
n Kum 29:20
o Isa 1:23; Eze 22:27; Mik 3:11
p Isa 7:8
q Mal 4:1
r Isa 5:24
s Eze 24:21
t Zb 31:14; Isa 7:13; Mik 7:7

u 2Fa 17:14; 2Nya 36:16; Yer 25:3; Zek 1:4; v Kum 28:64; Amo 9:9; **SURA 10** w Isa 5:1; Eze 15:6; x Zek 7:6.

kulingana na wingi wa matunda yake.[a] Wao huweka nguzo nzuri[b] kulingana na wema wa nchi yake. **2** Moyo wao umekuwa na unafiki;[c] sasa watapatikana na hatia.

"Kuna yule atakayevunja madhabahu zao; atapora nguzo zao.[d] **3** Kwa maana sasa watasema, 'Hatuna mfalme yeyote,[e] kwa kuwa hatukumwogopa Yehova. Naye mfalme atatufanyia nini?'

4 "Wao husema maneno, wakila viapo vya uwongo,[f] wakifanya agano;[g] na hukumu imechipuka kama mmea wenye sumu katika mitaro ya shamba.[h] **5** Wakaaji wa Samaria wataogopa kwa sababu ya sanamu ya ndama ya Beth-aveni;[i] kwa maana watu wake wataiombolezea, na vilevile makuhani wake wa miungu ya kigeni waliokuwa wakishangilia juu yake, kwa sababu ya utukufu wake, kwa maana itakuwa imeenda uhamishoni mbali nayo.[j] **6** Nayo itachukuliwa Ashuru na mtu fulani iwe zawadi kwa mfalme mkuu.[k] Efraimu naye atapata aibu,[l] na Israeli atalionea aibu shauri lake.[m] **7** Samaria na mfalme wake hakika watanyamazishwa,[n] kama tawi lililokatwa juu ya uso wa maji. **8** Na mahali pa juu pa Beth-aveni,[o] dhambi ya Israeli,[p] pataangamizwa. Miiba na mibaruti[q] itakuja juu ya madhabahu zao.[r] Na hakika watu wataiambia milima, 'Tufunikeni!' na vilima, 'Tuangukieni!'[s]

9 "Umetenda dhambi[t] kuanzia siku za Gibea,[u] Ee Israeli. Huko walisimama tuli. Vita juu ya wana wenye kukosa uadilifu katika Gibea havikupata kuwafikia.[a] **10** Wakati nitakapopenda nitawatia nidhamu pia.[b] Na vikundi vya watu vitakusanyika juu yao watakapofungwa pamoja na makosa yao mawili.[c]

11 "Na Efraimu alikuwa ndama-jike aliyezoezwa, anayependa kupura;[d] nami mwenyewe nikapita juu ya shingo yake yenye kupendeza. Nafanya mtu fulani ampande Efraimu.[e] Yuda hulima;[f] Yakobo humlimia.[g] **12** Mjipandie mbegu kwa uadilifu;[h] mvune kulingana na fadhili zenye upendo.[i] Mjilimie udongo unaofaa kwa kilimo,[j] kukiwa kungali na wakati wa kumtafuta Yehova mpaka atakapokuja[k] na kuwatolea ninyi mafundisho kwa uadilifu.[l]

13 "Ninyi mmelima uovu.[m] Nanyi mmevuna ukosefu wa uadilifu.[n] Mmekula matunda ya udanganyifu,[o] kwa maana mmetegemea njia yenu,[p] katika wingi wa watu wenu wenye nguvu.[q] **14** Na fujo imetokea kati ya watu wako,[r] na majiji yako yenye ngome yataporwa yote,[s] kama vile Shalmani alivyopora nyumba ya Arbeli, katika siku ya pigano ambapo mama mmoja alivunjwa vipande-vipande kando ya wanawe.[t] **15** Mtu fulani atawafanyia vivyo hivyo, Ee Betheli, kwa sababu ya ubaya wenu mwingi.[u] Hakika mfalme wa Israeli atanyamazishwa[v] wakati wa mapambazuko."

11 "Israeli alipokuwa mvulana, ndipo nikampenda,[w] na kutoka Misri nilimwita mwanangu.[x]

SURA 10

a Yer 2:28; Eze 6:13; Ho 8:11; Ho 12:11
b 1Fa 14:23; Ho 8:4
c 1Fa 18:21; Sef 1:5
d Yer 43:13; Mik 5:13; Zek 13:2
e Ho 3:4; Ho 13:11
f 2Fa 17:4; Eze 17:13
g Ho 6:7
h Kum 29:18; Isa 5:7; Amo 5:7; Amo 6:12
i 1Fa 12:28; Ho 4:15; Amo 3:14
j 1Sa 4:21
k 2Fa 17:3; Ho 5:13
l Yer 2:26; Yer 48:13; Eze 36:32
m Isa 30:3; Yer 7:24; Mik 6:16
n 2Fa 17:4
o Ho 4:15; Amo 7:9
p Kum 9:21; 1Fa 12:28; 1Fa 12:30; Mik 1:5
q Isa 32:13; Isa 34:13
r 2Fa 23:15
s Isa 2:19; Lu 23:30; Ufu 6:16
t Ho 9:9
u Amu 20:5

Safu ya 2

a Amu 20:19
b Ebr 12:6
c 1Fa 14:16; Eze 16:37
d Yer 50:11
e 2Fa 17:6
f Yer 4:3
g Isa 28:24
h Met 11:19; Yak 3:18
i Met 11:18
j Yer 4:3
k Isa 55:6; Amo 5:4
l Kum 32:2; Isa 45:8
m Ga 6:7
n Met 22:8; Ho 8:7
o Met 1:31
p Zb 52:7
q Zb 33:16; Zb 146:3; Yer 17:5
r Zb 74:23
s 2Fa 18:9; 2Fa 19:13
t Isa 13:16; Nah 3:10
u Amo 7:9
v 2Fa 18:10

SURA 11 w Kum 7:8; Yer 2:2; Eze 16:6; x Kut 4:22; Mt 2:15.

2 "Waliwaita.[a] Kwa kadiri
hiyohiyo walienda mbali kuto-
ka mbele yao.[b] Wakaanza ku-
toa dhabihu kwa sanamu za
Baali,[c] nao wakaanza kufuki-
za moshi wa dhabihu kwa sana-
mu za kuchongwa.[d] **3** Laki-
ni mimi, nilimfundisha Efrai-
mu kutembea,[e] nikawachukua
mikononi mwangu;[f] wala ha-
wakutambua kwamba nilikuwa
nimewaponya.[g] **4** Nilizi-
di kuwavuta kwa kamba za
mtu wa udongo, kwa kamba
za upendo,[h] hata nikawa kwao
kama wale wanaoondoa nira
kwenye mfupa wa mataya
yao,[i] nami kwa upole nikamle-
tea kila mmoja wao chaku-
la.[j] **5** Hatarudi katika nchi
ya Misri, bali Ashuru ataku-
wa mfalme wake,[k] kwa sababu
walikataa kurudi.[l] **6** Na upa-
nga utazunguka-zunguka kati-
ka majiji yake[m] na kukomesha
mapingo yake na kula[n] kwa sa-
babu ya mashauri yao.[o] **7** Na
watu wangu wanaelekea kuni-
kosea uaminifu.[p] Nao huwaita
kuelekea juu; wala hakuna ye-
yote anayesimama.

8 "Nawezaje kukuacha, Ee
Efraimu?[q] Nawezaje kukutoa,
Ee Israeli?[r] Nawezaje kukufa-
nya uwe kama Adma?[s] Naweza-
je kukuweka uwe kama Sebo-
iimu?[t] Moyo wangu umebadili-
ka ndani yangu;[u] na wakati huo-
huo huruma zangu zimewaka.
9 Sitaonyesha hasira yangu
inayowaka.[v] Sitaharibu tena
Efraimu,[w] kwa maana mimi ni
Mungu,[x] mimi si mwanadamu,
mimi ndiye Mtakatifu katikati
yako;[y] wala sitakuja nikiwa na
hasira. **10** Watatembea kwa
kumfuata Yehova.[z] Atangurum-
a kama simba;[a] kwa maana
yeye mwenyewe atanguruma,[a]
na wana watakuja wakitetemeka
kutoka upande wa magharibi.[b] **11** Watakuja kutoka Misri[c] wakitetemeka kama nde-
ge, na kama njiwa kutoka nchi
ya Ashuru;[d] nami nitawafanya
wakae katika nyumba zao,"
asema Yehova.[e]

12 "Efraimu amenizunguka
kwa maneno ya uwongo,[f] na
nyumba ya Israeli kwa udanganyifu. Lakini Yuda bado anatembea pamoja na Mungu,[g] naye
ni mwaminifu kwa aliye Mtakatifu Zaidi."

12 "Efraimu anajilisha upe-
po[h] na kufukuza upepo
wa mashariki siku nzima.[i] Anazidisha uwongo na uporaji.[j]
Nao hufanya agano na Ashuru,[k] na mafuta hupelekwa Misri.

2 "Naye Yehova ana kesi
na Yuda,[l] kumtoza Yakobo hesabu kulingana na njia zake;[m]
atamlipa kulingana na matendo yake.[n] **3** Alimkamata
ndugu yake kwenye kisigino
ndani ya tumbo,[o] na kwa ngu-
vu zake zenye msukumo alishindana na Mungu.[p] **4** Akaendelea kushindana na malaika,
naye mwishowe akashinda.[q]
Alilia, ili apate kujiombea kibali kwa bidii."[r]

Alimkuta Betheli,[s] na huko
Yeye akaanza kusema nasi.[t]
5 Na Yehova Mungu wa majeshi,[u] Yehova ni ukumbusho
wake.[v]

6 "Na wewe inakupasa kuru-
di kwa Mungu wako,[w] ushike

SURA 11
a Kum 29:2; 2Nya 36:15; Zek 1:4
b 2Nya 36:16; Isa 30:9
c Amu 2:13; Amu 3:7; 1Fa 16:31; 1Fa 18:19; 2Fa 17:16; Ho 2:13
d 1Fa 12:33; Isa 65:7; Yer 18:15; Ho 13:2
e Kum 8:2
f Kum 1:31; Kum 33:27; Isa 40:11; Isa 46:3; Isa 63:9
g Kut 15:26; Zb 103:3; Isa 30:26
h 2Sa 7:14; Isa 63:9; Yoh 6:44
i Law 26:13
j Zb 78:24; Zb 105:40
k 2Fa 17:3
l 2Fa 17:13; Yer 8:5; Amo 4:6
m Law 26:31; Yer 5:17
n Eze 20:47; Mal 4:1
o Isa 30:1
p Zb 78:57; Yer 3:6; Yer 8:5
q Ho 6:4
r Yer 9:7
s Mwa 10:19; Kum 29:23
t Mwa 14:8
u Kum 32:36; Yer 31:20
v Zb 78:38
w Yer 30:11
x Hes 23:19; Isa 55:8; Mal 3:6
y Isa 12:6
z Isa 2:5
a Isa 31:4

Safu ya 2
a Yoe 3:16; Amo 1:2
b Zek 8:7
c Isa 11:11; Zek 10:10
d Isa 11:12; Isa 60:8
e Yer 23:6; Eze 28:25; Eze 37:21; Amo 9:14
f Zb 78:36; Isa 29:13; Mik 6:12
g 2Fa 18:5; 2Nya 29:2; Zb 89:18; Ho 4:15

SURA 12
h Yer 22:22
i Ho 8:7
j 2Fa 17:4
k 2Fa 15:19
l 2Fa 17:19; Yer 2:35; Ho 4:1; Mik 6:2; m Zb 62:12; Yer 17:10; n Isa 3:11; Isa 59:18; o Mwa 25:26; p Mwa 32:28; q Mwa 32:25; r Mwa 32:26; s Mwa 28:19; t Mwa 28:13; u Mwa 28:16; Mwa 32:30; v Kut 3:15; Zb 135:13; Isa 42:8; w Isa 31:6; Yer 3:14; Ho 14:1; Yoe 2:13; Zek 1:3.

fadhili zenye upendo[a] na haki;[b]
nawe umtumaini Mungu wako
sikuzote.[c] **7** Mfanya-biashara ana mizani ya udanganyifu mkononi mwake;[d] amependa
kupunja.[e] **8** Na Efraimu anaendelea kusema, 'Kwa kweli nimekuwa tajiri;[f] nimejipatia vitu
vyenye thamani.[g] Na kuhusu
kazi yangu yote ya kutaabika,
hawatanipata nikiwa na kosa lililo dhambi.'[h]
9 "Lakini mimi ni Yehova
Mungu wako kuanzia nchi
ya Misri.[i] Na bado nitakufanya
ukae katika mahema kama katika siku za wakati uliowekwa.
10 Nami nilisema na manabii,[j]
nikazidisha maono, nikaendelea kutoa mifano kupitia mkono
wa manabii.[k]
11 "Mambo ya uchawi,[l] pia
yasiyo ya kweli,[m] yametokea
Gileadi. Wametoa dhabihu za
ng'ombe katika Gilgali.[n] Zaidi ya hayo, madhabahu zao ni
kama mafungu ya mawe katika matuta ya shamba.[o] **12** Na
Yakobo akakimbia kwenda katika nchi ya Siria,[p] na Israeli[q] akaendelea kutumikia apate mke,[r] naye akalinda kondoo
apate mke.[s] **13** Na Yehova
kupitia nabii akaleta Israeli
kutoka Misri,[t] naye akalindwa
kupitia nabii.[u] **14** Efraimu
alichukiza akatia uchungu,[v]
na matendo yake ya kumwaga damu anayaacha juu yake
mwenyewe,[w] na Bwana-Mkuu
wake atamlipa yeye shutuma
zake."[x]

13 "Efraimu aliposema, alitetemesha; yeye alichukuliwa kwa uzito katika Israeli.[y] Lakini akawa na hatia
kuhusiana na Baali,[z] akafa.[a]
2 Na sasa wanafanya dhambi
zaidi na kujifanyia sanamu ya
kuyeyushwa kutoka kwenye
fedha[a] yao, sanamu kulinganana na uelewaji wao wenyewe,[b]
yote hiyo ni kazi ya mafundi.[c]
Nao wanaziambia, 'Acheni wanadamu wanaotoa dhabihu wabusu ndama.'[d] **3** Kwa hiyo
watakuwa kama mawingu ya
asubuhi[e] na kama umande unaotoweka mapema; kama makapi yanayopeperushwa mbali
kutoka kwenye uwanja wa kupuria[f] na kama moshi kutoka
katika tundu la paa.
4 "Lakini mimi ni Yehova Mungu wako kuanzia nchi ya Misri,[g]
wala hukuwa unamjua Mungu
mwingine yeyote ila mimi; wala
hapakuwa na mwokozi mwingine yeyote ila mimi.[h] **5** Mimi
mwenyewe nilikujua wewe nyikani,[i] katika nchi yenye homa
nyingi.[j] **6** Pia wakashiba kulingana na malisho yao.[k] Walishiba, kisha moyo wao ukaanza kujiinua.[l] Ndiyo sababu walinisahau mimi.[m] **7** Nami nitakuwa
kwao kama mwana-simba.[n] Nitaendelea kutazama kama chui
kando ya njia.[o] **8** Nitakutana
nao kama dubu ambaye amepoteza watoto wake,[p] nitaurarua ukuta wa moyo wao. Nami
nitawala hapo kama simba;[q]
mnyama wa mwituni atawararua vipande-vipande.[r] **9** Hakika atakuharibu wewe,[s] Ee
Israeli, kwa sababu ilikuwa juu
yangu, juu ya msaidizi wako.[t]
10 "Basi, yuko wapi mfalme
wako, apate kukuokoa katika majiji yako yote,[u] na waamuzi wako, ambao ulisema hivi

SURA 12

a Mik 6:8
b Kum 16:20
c Zb 27:14 Omb 3:25
d Law 19:35 Met 11:1 Amo 8:5
e Eze 22:29 Mik 2:1
f Met 28:20 Yer 9:23 Zek 11:5 Ufu 3:17
g Kum 8:17
h Met 30:12 Mal 2:17
i Kut 20:2 Ho 13:4
j 1Fa 17:1 2Fa 17:13 Amo 7:15
k Isa 5:1 Yer 13:1
l Ho 6:8
m Eze 13:8
n Amo 4:4
o 2Fa 17:10 Ho 8:11
p Mwa 28:5 Kum 26:5
q Mwa 32:28
r Mwa 29:18
s Mwa 31:38
t Kut 12:51 Zb 77:20 Isa 63:11 Mik 6:4
u Yos 24:17 1Sa 12:8
v 2Fa 17:11 Eze 23:5
w Eze 22:13
x Kum 28:37 Ro 2:6

SURA 13

y Yos 17:17
z 2Fa 17:16 Ho 11:2
a Kut 20:5

Safu ya 2

a Zb 115:4 Isa 46:6 Yer 10:4 Ho 2:8
b Isa 44:17 Yer 10:9
c Yer 10:3 Hab 2:18
d 1Fa 12:28 1Fa 19:18
e Ho 6:4
f Ayu 21:18 Zb 1:4 Da 2:35
g Kut 20:2 Law 11:45 Zb 81:10 Ho 12:9
h Isa 43:11 Isa 45:21
i Kum 2:7 Kum 32:10 Yer 2:2
j Yer 2:6
k Kum 8:12 Ne 9:25
l Kum 32:15

m Kum 6:12; Kum 32:18; Met 30:9; Isa 17:10; n Ho 5:14; o Yer 5:6; p 2Sa 17:8; Met 17:12; q Omb 3:10; r Isa 56:9; Yer 12:9; s Met 6:32; t Zb 33:20; Zb 46:1; u 1Sa 8:20; 2Fa 17:4.

kuwahusu, ‘Nipe mfalme na wakuu’?[a] **11** Ndipo nilikupa mfalme katika hasira yangu,[b] nami nitamwondolea mbali katika ghadhabu yangu.[c]

12 “Kosa la Efraimu limefungwa, dhambi yake imewekwa akiba kama hazina.[d] **13** Uchungu wa mwanamke anayezaa utamshika yeye.[e] Yeye ni mwana asiye na hekima,[f] kwa maana katika majira yake, hatasimama wakati wana watakapotoka katika tumbo la uzazi.[g]

14 “Nitawakomboa wao kutoka katika mkono wa Kaburi;*[h] nitawaokoa wao[i] kutoka kwenye kifo. Ee Kifo, iko wapi michomo yako?[j] Ee Kaburi,# yako wapi maangamizi yako?[k] Huruma itafichwa kutoka machoni pangu.[l]

15 “Hata yeye akizaa sana[m] kama mimea ya matete, upepo wa mashariki, upepo wa Yehova, utakuja.[n] Unakuja kutoka nyikani, nao utakausha kisima chake na kukausha bubujiko lake.[o] Huyo atapora hazina ya vyombo vyote vyenye kutamanika.[p]

16 “Samaria atahesabiwa kuwa na hatia,[q] kwa maana kwa kweli yeye amemwasi Mungu wake.[r] Wataanguka kwa upanga.[s] Watoto wao wenyewe watavunjwa vipande-vipande,[t] na wanawake wao wenye mimba watapasuliwa.”[u]

14 “Ee Israeli, rudi kwa Yehova Mungu wako,[v] kwa maana umejikwaa katika kosa lako.[w] **2** Chukueni maneno pamoja nanyi mrudi kwa Yehova.[x] Mwambieni hivi, enyi nyote, ‘Samehe kosa letu;[a] na ukubali lililo jema, nasi tutatoa ng’ombe-dume wachanga wa midomo yetu.[b] **3** Ashuru yenyewe haitatuokoa.[c] Hatutapanda farasi.[d] Na hatutaiambia tena kazi ya mikono yetu: “Ee Mungu wetu!” kwa sababu ni kupitia wewe kwamba mvulana asiye na baba huonyeshwa rehema.’[e]

4 “Nitaponya ukosefu wao wa uaminifu.[f] Nitawapenda kwa kupenda kwangu mwenyewe,[g] kwa maana hasira yangu imegeuka kutoka kwake.[h] **5** Nitakuwa kama umande kwa Israeli.[i] Atachanua kama yungiyungi, na kueneza mizizi yake kama mti wa Lebanoni. **6** Matawi yake yatasambaa, na utukufu wake utakuwa kama ule wa mzeituni,[j] na harufu yake nzuri itakuwa kama ile ya mti wa Lebanoni. **7** Watakaa tena katika kivuli chake.[k] Watakuza nafaka, nao watachipuka kama mzabibu.[l] Ukumbusho wake utakuwa kama divai ya Lebanoni.

8 “Efraimu atasema, ‘Nina nini tena na sanamu?’[m]

“Hakika mimi mwenyewe nitatoa jibu, nami nitaendelea kumtazama.[n] Mimi ni kama mberoshi wenye majani mengi.[o] Matunda kwa ajili yako yatapatikana kwangu.”

9 Ni nani aliye na hekima, apate kuelewa mambo haya?[p] Mwenye busara, apate kuyajua?[q] Kwa maana njia za Yehova zimenyooka,[r] na waadilifu ndio watakaotembea katika hizo;[s] bali wakosaji ndio watakaojikwaa katika hizo.[t]

SURA 13
a 1Sa 8:5
b 1Sa 8:7
1Sa 12:13
c 1Sa 12:25
Yer 52:11
d Kum 32:34
Ayu 14:17
e Yer 30:6
Mik 4:9
f Met 22:3
g 2Fa 19:3
h Zb 30:3
Zb 49:15
Zb 69:18
i Isa 25:8
j Isa 26:19
1Ko 15:55
k Ufu 20:13
l 1Sa 15:29
Yer 15:6
m Mwa 41:52
Mwa 48:19
n Yer 4:11
Ho 4:19
o Ho 9:11
p 2Fa 17:20
q 2Fa 17:18
Amo 3:9
r 1Sa 15:23
Zb 5:10
Eze 20:21
s Isa 1:20
Isa 7:8
t 2Fa 8:12
u 2Fa 15:16
Amo 1:13

SURA 14
v 1Sa 7:3
2Nya 30:6
Isa 55:6
Ho 12:6
Yoe 2:13
w Yer 2:19
Omb 4:6
x Ho 12:6

Safu ya 2
a Kut 34:7
2Sa 24:10
Zb 51:2
Mik 7:18
b Zb 69:31
Ebr 13:15
c Ho 5:13
d Kum 17:16
Zb 33:17
Isa 31:1
e Kum 10:18
Zb 10:14
Zb 68:5
Zb 146:9
Met 23:11
Yak 1:27
f Zb 103:3
Isa 57:18
Yer 3:22
g Kum 7:7
Sef 3:17
h Zb 78:38
Isa 12:1
i Kum 32:2
Met 19:12
j Zb 52:8
k Zb 91:1
l Zek 8:12
m Ho 14:3
Mdo 19:18
n Yer 31:18
o Isa 41:19
Isa 55:13
Isa 60:13

Ho 13:14* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.
14# Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

p Zb 107:43; Met 1:5; Yer 9:12; q Mt 24:45; r Kum 32:4; Da 4:37; s Lu 1:6; t Da 12:10.

YOELI

1 Neno la Yehova lililomjia[a]
Yoeli mwana wa Pethueli:
2 "Sikieni jambo hili, ninyi
wanaume wazee, tegeni sikio,
ninyi wakaaji wote wa nchi.[b] Je,
hili limetokea katika siku zenu,
au hata katika siku za mababu zenu?[c] **3** Kuhusu hilo wa-
simulieni wana wenu wenye-
we, nao wawasimulie wana wao,
nao wana wao wasimulie kizazi
kinachofuata.[d] **4** Kilichoa-
chwa na kiwavi, nzige ame-
kula;[e] kilichoachwa na nzige,
nzige mchanga amekula; kili-
choachwa na nzige mchanga,
mende amekula.[f]
5 "Amkeni, ninyi walevi,[g] li-
eni; pigeni mayowe,[h] ninyi nyo-
te wanywaji wa divai, kwa saba-
bu ya divai tamu,[i] kwa maana
imekatiliwa mbali kutoka kati-
ka vinywa vyenu.[j] **6** Kwa ma-
ana kuna taifa ambalo limei-
ngia katika nchi yangu, lenye
nguvu nalo halihesabiki.[k] Meno
yake ni meno ya simba,[l] nalo
lina mifupa ya mataya ya si-
mba. **7** Limefanya mzabibu
wangu kuwa kitu cha kusha-
ngaza,[m] na mtini wangu kuwa
kisiki.[n] Limeumenya na kuutu-
pilia mbali.[o] Matawi yake yame-
kuwa meupe. **8** Ombolezeni,
kama bikira aliyevikwa nguo
za magunia[p] anavyoomboleza
kwa ajili ya mume wa ujana
wake.
9 "Toleo la nafaka[q] na to-
leo la kinywaji[r] limekatiliwa
mbali kutoka katika nyumba
ya Yehova; makuhani, walio
wahudumu[s] wa Yehova, wa-
meomboleza.[t] **10** Shamba li-
meporwa,[a] nchi imeomboleza;[b]
kwa maana nafaka imeporwa,
divai mpya imekauka,[c] mafuta
yamekauka.[d] **11** Wakulima
wameona aibu;[e] watunza-mi-
zabibu wamepiga mayowe, kwa
sababu ya ngano na kwa saba-
bu ya shayiri; kwa maana ma-
vuno ya shamba yameangami-
zwa.[f] **12** Mzabibu umekauka,
na hata mtini umedhoofika.
Nao mkomamanga, pia mtende
na mtofaa, miti yote ya sha-
mba imekauka;[g] kwa maana fu-
raha imetoweka kwa aibu kati-
ka binadamu.[h]
13 "Jifungeni mshipi, jipi-
geni vifua,[i] ninyi makuhani.
Pigeni mayowe, ninyi wahu-
dumu wa madhabahu.[j] Ingi-
eni ndani, kaeni usiku kucha
mkiwa mmevaa nguo za magu-
nia, ninyi wahudumu wa Mu-
ngu wangu; kwa maana nyu-
mba ya Mungu wenu imenyi-
mwa toleo la nafaka[k] na toleo
la kinywaji.[l] **14** Takaseni wa-
kati wa kufunga.[m] Iteni kusa-
nyiko kuu.[n] Kusanyeni pamoja
wanaume wazee, wakaaji wote
wa nchi, kwenye nyumba ya
Yehova Mungu wenu,[o] mlilieni
Yehova awape msaada.[p]
15 "Ole wake siku ile;[q] kwa
sababu siku ya Yehova iko ka-
ribu,[r] nayo itakuja kama mpo-
raji kutoka kwa Mweza-Yote!
16 Je, chakula hakijakatiliwa
mbali mbele ya macho yetu;
kushangilia na furaha kuto-
ka katika nyumba ya Mungu
wetu?[s] **17** Tini zilizokaushwa
zimenyauka chini ya sepetu
zake. Maghala yamefanywa

SURA 1

a 2Pe 1:21
b Zb 49:1
Amo 3:1
c Yoe 2:2
d Kut 10:14
Kut 13:14
Kum 6:7
Kum 29:22
Zb 78:4
e Kut 10:15
Kum 28:38
Amo 4:9
f Yoe 2:25
g Isa 28:1
Amo 6:6
Lu 21:34
h Yer 4:8
Yak 5:1
i Ho 4:11
j Kum 28:39
Isa 32:10
k Yoe 2:2
l Ufu 9:8
m Isa 5:6
n Yer 5:17
Yer 8:13
o Yer 48:32
p Eze 7:18
q Law 2:1
Yoe 2:14
r Kut 29:40
Ho 9:4
s 2Nya 13:10
t Yoe 2:17

Safu ya 2

a Kum 28:30
b Law 26:20
Yer 4:28
Yer 14:2
c Kum 28:39
Isa 24:7
Ho 9:2
d Kum 28:40
e Yer 14:4
f Isa 17:11
g Law 26:20
h Isa 24:11
i Yer 4:8
Eze 7:18
j Kut 30:20
1Ko 9:13
k Law 2:8
l Hes 29:6
m 2Nya 20:3
Yoe 2:15
n Law 23:36
Ne 8:18
o 2Nya 20:13
Ne 9:1
p Kum 4:30
Zb 50:15
Yon 3:8
q Yer 30:7
r Isa 13:6
Yoe 2:1
Sef 1:7
Sef 1:14
Sef 2:2
2Pe 3:10
Ufu 6:17
s Kum 12:7

ukiwa. Mabanda yamebomolewa, kwa maana nafaka imekauka. **18** Lo! Jinsi mnyama wa
kufugwa ameugua! Jinsi makundi ya ng'ombe yamevurugika! Kwa maana hawana malisho.[a] Pia, makundi ya kondoo
ndiyo yamefanywa yachukue hatia.

19 "Nitakuita wewe, Ee Yehova;[b] kwa maana moto umeteketeza malisho ya nyikani,
na mwali wa moto umeteketeza miti yote ya mwituni.[c] **20** Wanyama wa mwituni pia
wanakutamani wewe,[d] kwa sababu mifereji ya maji imekauka,[e] na moto umeteketeza malisho ya nyikani."

2 "Pigeni baragumu katika
Sayuni,[f] pigeni kelele za
vita[g] katika mlima wangu mtakatifu.[h] Wakaaji wote wa nchi
na wafadhaike;[i] kwa maana
siku ya Yehova inakuja,[j] kwa
maana iko karibu! **2** Siku
hiyo ni siku yenye giza na weusi, siku yenye mawingu na weusi mzito,[k] kama nuru ya mapambazuko iliyotandazwa juu ya milima.[l]

"Kuna kundi la watu wengi
sana na wenye nguvu;[m] kundi
kama hilo halijapata kuwako
tangu zamani za kale,[n] wala baada yake hakutakuwa na lingine tena hata kwa miaka ya kizazi baada ya kizazi. **3** Mbele
yake moto umeteketeza,[o] na
nyuma yake mwali wa moto
huteketeza.[p] Mbele yake nchi
ni kama bustani ya Edeni;[q] lakini nyuma yake ni nyika iliyo
ukiwa, wala hakuna chochote
kinachoponyoka.

4 "Sura yake ni kama sura
ya farasi, nao hukimbia kama

SURA 1

a 1Fa 18:5
Yer 12:4
Ho 4:3
b Zb 50:15
Zb 91:15
Mik 7:7
Hab 3:18
Flp 4:6
c Yer 9:10
d Ayu 38:41
Zb 104:21
Zb 145:15
Zb 147:9
e 1Fa 17:7
1Fa 18:5
Yer 14:1

SURA 2

f Yer 4:5
Eze 33:3
g Sef 1:16
h Zek 8:3
i Amo 3:6
j Sef 1:14
Mal 4:1
k Yer 4:28
Yer 13:16
Amo 5:18
l Amo 4:13
Sef 1:15
m Yoe 1:6
n Kut 10:14
o Yoe 1:19
p Amo 7:4
q Mwa 2:8
Mwa 13:10
Isa 51:3

Safu ya 2

a Ufu 9:7
b Ufu 9:9
c Isa 5:24
d Met 30:27
e Yer 8:21
f Nah 2:10
g 2Sa 1:23
h Met 30:27
i Yer 4:28
Yoe 2:31
Mt 24:29
Lu 21:25
Mdo 2:20
Ufu 9:2
j Isa 13:10
k Zb 46:6
Isa 42:13
Yer 25:30
Yoe 3:16
Amo 1:2
l Yoe 2:25
m Yoe 2:2
n Yer 30:7
Amo 5:18
Sef 1:15
o Hes 24:23
Nah 1:6
Ufu 6:17
p Yer 4:1
Ho 12:6
Ho 14:1
q 1Sa 7:6
2Nya 20:3
r Ezr 10:1
Isa 22:12
Yak 4:9
s 2Fa 22:19
Zb 34:18
Zb 51:17
Isa 57:15

farasi wa vita.[a] **5** Wao hurukaruka kama kwa sauti ya magari juu ya vilele vya milima,[b]
kama kwa sauti ya mwali wa
moto ambao unateketeza majani makavu.[c] Wao ni kama kundi la watu wenye nguvu, lililowekwa katika mpangilio wa
pigano.[d] **6** Vikundi vya watu
vitakuwa na maumivu makali
kwa sababu yake.[e] Nazo nyuso
zote zitakuwa na wasiwasi.[f]

7 "Wanakimbia kama wanaume wenye nguvu.[g] Wanapanda ukuta kama wanaume wa
vita. Nao huenda kila mmoja katika njia zake, nao hawabadili mapito yao.[h] **8** Wala
hawasukumani. Wanasonga
mbele kama mwanamume katika mwendo wake; na baadhi
yao wakianguka katikati ya silaha, wale wengine hawageuzi mwendo wao.

9 "Wao huvuma kuingia jijini. Hukimbia ukutani. Hupanda juu ya nyumba. Wanaingia
kupitia madirisha kama mwizi. **10** Mbele yao nchi imefadhaishwa, mbingu zimetikisika. Jua na mwezi zimekuwa
na giza,[i] na nyota zimeondoa
mwangaza wake.[j] **11** Naye
Yehova atatoa sauti yake[k]
mbele ya jeshi lake,[l] kwa maana kambi yake ina watu wengi
sana.[m] Kwa maana yeye anayelitimiza neno lake ni mwenye
nguvu; maana siku ya Yehova
ni kuu[n] na yenye kuogopesha
sana, naye ni nani anayeweza
kustahimili mbele yake?"[o]

12 "Na sasa pia," asema Yehova, "rudini kwangu kwa mioyo yenu yote,[p] kwa kufunga,[q]
kwa kulia, na kwa kuomboleza.[r] **13** Irarueni mioyo yenu,[s]

wala si mavazi yenu;[a] rudini kwa Yehova Mungu wenu,
kwa maana yeye ana neema
na rehema,[b] si mwepesi wa
hasira[c] naye ni mwingi wa fa-
dhili zenye upendo,[d] naye haki-
ka atajuta kwa sababu ya msi-
ba huo.[e] **14** Ni nani anayejua
ikiwa yeye hatageuka na kuju-
ta[f] na baada ya hayo abakize
baraka,[g] toleo la nafaka na to-
leo la kinywaji kwa ajili ya Ye-
hova Mungu wenu?

15 "Pigeni baragumu katika Sayuni.[h] Takaseni wakati wa kufunga.[i] Iteni kusanyiko kuu.[j] **16** Kusanyeni watu pamoja. Takaseni kutaniko.[k] Kusanyeni wazee. Kusanyeni pamoja watoto na wale wanaonyonya.[l] Bwana-arusi na atoke katika chumba chake cha ndani, bibi-arusi naye atoke katika chumba chake cha ndoa.

17 "Makuhani, walio wahudumu wa Yehova, na walie kati ya ukumbi na madhabahu,[m] wakisema, 'Ee Yehova, wasikitikie watu wako, usiufanye urithi wako kuwa shutuma,[n] mataifa wawatawale. Kwa nini waseme kati ya makabila ya watu: "Yuko wapi Mungu wao?"'[o] **18** Yehova atakuwa mwenye bidii kwa ajili ya nchi yake[p] naye atawaonea huruma watu wake.[q] **19** Yehova atajibu na kuwaambia watu wake, 'Tazama nawapelekea ninyi nafaka na divai mpya na mafuta, nanyi mtaishiba;[r] nami sitawafanya tena kamwe kuwa shutuma kati ya mataifa.[s] **20** Na mkaaji wa kaskazini[t] nitamweka mbali kabisa kutoka juu yenu, nami nitamtawanya yeye katika nchi isiyo na maji na iliyo ukiwa, uso wake ukiwa kwenye bahari ya mashariki[a] na upande wake wa nyuma kwenye bahari ya magharibi.[b] Na uvundo kutoka kwake utapanda, na mnuko kutoka kwake utazidi kupanda;[c] kwa maana Yeye atafanya jambo kuu katika yale ambayo Yeye hufanya.'

21 "Usiogope, Ee nchi. Shangilia na ufurahi; kwa maana Yehova atafanya jambo kuu katika yale ambayo Yeye hufanya.[d] **22** Msiogope, ninyi wanyama wa mwituni,[e] kwa maana malisho ya nyikani yatatota majani mabichi.[f] Kwa maana mti utatokeza matunda yake.[g] Mtini na mzabibu itatokeza nguvu zake.[h] **23** Nanyi, wana wa Sayuni, furahini na mshangilie katika Yehova Mungu wenu;[i] kwa maana atakuwa na wajibu wa kuwapa mvua ya vuli kwa kiasi kinachofaa,[j] naye atawaletea ninyi mvua kubwa, mvua ya vuli na mvua ya masika, kama pale mwanzoni.[k] **24** Na viwanja vya kupuria vitajaa nafaka iliyosafishwa, na mitungi ya mashinikizo itafurika kwa divai mpya na mafuta.[l] **25** Nami nitawalipa ninyi ridhaa kwa sababu ya miaka ambayo nzige, nzige mchanga, na mende na kiwavi wamekula, jeshi langu kubwa ambalo nimetuma kati yenu.[m] **26** Nanyi mtakula, mle na kushiba,[n] nanyi mtalisifu jina la Yehova Mungu wenu,[o] ambaye amewatendea kwa njia ya ajabu;[p] na watu wangu hawataona aibu mpaka wakati usio na kipimo.[q] **27** Nanyi mtajua ya kuwa

SURA 2

a Mwa 37:34; 2Sa 1:11
b Kut 34:6; Mik 7:19
c Hes 14:18; Isa 48:9; Mik 7:18; Nah 1:3
d Ne 9:17; Zb 86:15; Zb 103:8; Yon 4:2
e Zb 106:45
f 2Nya 30:8; Yer 18:8; Yon 3:9; Sef 2:3
g Isa 65:8; Mik 7:20; Hag 2:19
h Yoe 2:1
i Yer 36:9; Yoe 1:14
j 2Nya 7:9
k Kut 19:10
l Kum 29:11; Kum 31:12; 2Nya 20:13
m 2Nya 8:12; Mt 23:35
n Kum 28:37; Zb 44:14
o Kum 32:27; Zb 42:10; Zb 79:10; Zb 115:2; Mik 7:10
p Zek 1:14; Zek 8:2
q Kum 32:36; Zb 103:13; Isa 60:10; Omb 3:22; Ho 11:8; Lu 15:20; Yak 5:11
r Isa 62:8; Amo 9:13; Mal 3:10
s Eze 34:29; Eze 36:15
t Yer 1:14

Safu ya 2

a Eze 47:18
b Kum 11:24; Kum 34:2
c Isa 34:3
d Zb 126:3
e Zb 36:6
f Zb 65:12; Isa 30:23; Zek 8:12
g Zb 67:6; Isa 51:3; Eze 34:27
h Amo 9:14
i Zb 28:7; Isa 12:6; Isa 41:16; Isa 61:10; Hab 3:18; Zek 10:7
j Law 26:4
k Kum 11:14; Zek 10:1; Yak 5:7
l Law 26:10; Met 3:10; Amo 9:13; Mal 3:10
m Yoe 1:4; Amo 4:9
n Law 26:5; Kum 6:11; Zb 22:26;
o Kum 26:10;
p Zb 13:6; Zb 72:18; Isa 25:1;
q Zb 37:19; Sef 3:11; Ro 5:5.

mimi nimo katikati ya Israeli,[a] na kwamba mimi ni Yehova Mungu wenu wala hakuna mwingine.[b] Na watu wangu hawataona aibu sikuzote.

28 "Kisha itakuwa kwamba nitaimimina roho yangu[c] juu ya kila namna ya mwili,[d] na wana wenu na binti[e] zenu watatoa unabii. Nao wazee wenu wataota ndoto. Nao wanaume wenu vijana wataona maono. **29** Na hata juu ya watumishi wa kiume na juu ya wajakazi katika siku hizo nitaimimina roho yangu.[f]

30 "Nami nitatoa maajabu mbinguni[g] na duniani, damu na moto na nguzo za moshi.[h] **31** Jua litageuzwa kuwa giza,[i] na mwezi kuwa damu,[j] kabla ya kuja kwa ile siku ya Yehova iliyo kuu na yenye kuogopesha.[k] **32** Na itakuwa kwamba kila mtu anayeliitia jina la Yehova ataokoka;[l] kwa maana katika Mlima Sayuni na katika Yerusalemu kutakuwako wale waliokoponyoka,[m] kama vile ambavyo Yehova amesema, na kati ya waokokaji, ambao Yehova anaita."[n]

3 "Kwa maana, tazama! siku hizo na wakati huo,[o] nitakapowarudisha mateka wa Yuda na Yerusalemu,[p] **2** mimi pia nitayakusanya pamoja mataifa yote[q] na kuwaleta kwenye bonde la Yehoshafati;[r] nami huko nitajiweka katika hukumu nao kwa sababu ya watu wangu na urithi wangu Israeli,[s] ambao wamewatawanya katikati ya mataifa; nao waligawanya nchi yangu mwenyewe.[t] **3** Nao waliwapigia kura watu wangu;[u] nao walikuwa wakimtoa mtoto wa kiume ili kumpata kahaba,[a] walimuuza mtoto wa kike wapate divai ili wanywe.

4 "Pia, mna nini nami, enyi Tiro na Sidoni[b] pia nanyi maeneo ya Ufilisti?[c] Je, hivyo ndivyo mnavyonitendea kwa kunipa thawabu? Na ikiwa mnanitendea hivyo, matendo yenu nitayalipa haraka, naam, upesi, juu ya vichwa vyenu.[d] **5** Kwa sababu ninyi mmechukua fedha yangu mwenyewe na dhahabu yangu,[e] nanyi mmeleta vitu vyangu vilivyo vyema katika mahekalu yenu;[f] **6** na wana wa Yuda na wana wa Yerusalemu mmewauza[g] kwa wana wa Wagiriki,[h] kwa kusudi la kuwaondolea mbali kutoka eneo lao wenyewe;[i] **7** tazama, ninawaamsha waje kutoka mahali ambapo mmewauza,[j] na matendo yenu nitayalipa juu ya vichwa vyenu wenyewe.[k] **8** Nami nitawauza wana wenu na binti zenu mikononi mwa wana wa Yuda,[l] nao watawauza kwa watu wa Sheba,[m] taifa lililo mbali;[n] kwa maana Yehova amesema hayo.

9 "Tangazeni mambo haya kati ya mataifa,[o] 'Takaseni vita! Amsheni wanaume wenye nguvu![p] Waacheni wakaribie! Na waje, wanaume wote wa vita![q] **10** Fueni majembe yenu yawe panga na miundu[r] yenu iwe mikuki. Aliye dhaifu na aseme: "Mimi ni mwanamume mwenye nguvu."[s] **11** Toeni msaada wenu na mje, enyi mataifa yote jirani,[t] mkusanyike pamoja.'"[u]

SURA 2
a Law 26:11; Zb 46:5; Eze 37:26
b Kum 4:35; 1Fa 8:60; Isa 45:5
c Isa 32:15; Isa 44:3; Eze 39:29; Mdo 2:17
d Zek 12:10; Yoh 7:39; Mdo 10:45
e Mdo 21:9
f Mdo 2:18
g Mdo 2:19
h Ufu 9:2
i Mdo 2:20
j Isa 13:10; Yoe 3:15; Mt 24:29; Mk 13:24; Lu 21:25; Ufu 6:12
k Sef 1:14; Mal 4:5
l Zb 50:15; Mdo 2:21; Ro 10:13
m Isa 46:13; Oba 17
n Isa 11:11; Yer 31:7; Mik 4:7; Ro 9:27

SURA 3
o Yer 30:3; Eze 38:14; Sef 3:20
p Kum 30:3; Yer 16:15; Eze 39:28; Amo 9:14
q Sef 3:8; Zek 14:2; Ufu 16:16
r Yoe 3:12
s Isa 66:16; Eze 38:22
t Yer 12:14; Eze 35:10; Sef 2:8
u Oba 11

Safu ya 2
a Kum 23:17
b Isa 23:12; Zek 9:2
c Yer 47:4; Eze 25:15
d Amo 1:10; Ro 2:6
e 2Nya 21:17
f 1Sa 5:2
g Kum 28:32; Eze 27:13
h Mwa 10:2; Zek 9:13
i Kum 28:68
j Isa 11:12; Isa 43:5; Isa 49:12; Yer 23:8; Eze 34:12
k Zb 62:12; Yer 17:10; Yer 25:14; Yer 30:23
l Oba 20
m Ayu 1:15; Eze 27:22
n Yer 6:20
o Isa 34:1; Yer 31:10; p Isa 8:9; Yer 46:3; q Eze 38:7; r Isa 2:4; Mik 4:3; s Zek 12:8; t Eze 38:9; Sef 3:8; u Ufu 16:14.

Mahali pale, Ee Yehova, uwashushe watu wako wenye nguvu.[a]

12 "Mataifa na yaamshwe, yaje kwenye bonde la Yehoshafati;[b] kwa maana hapo nitaketi ili kuhukumu mataifa yote yanayozunguka pande zote.[c]

13 "Tieni ndani mundu,[d] kwa maana mavuno yameiva.[e] Njooni, teremkeni, kwa maana shinikizo la divai limejaa.[f] Mitungi ya shinikizo inafurika; kwa maana ubaya wao umekuwa mwingi.[g] **14** Umati, umati umo katika bonde la uamuzi,[h] kwa maana siku ya Yehova iko karibu katika bonde la uamuzi.[i] **15** Jua na mwezi vitakuwa giza, na nyota zitaondoa mwangaza wake.[j] **16** Na kutoka Sayuni Yehova atanguruma, kutoka Yerusalemu atatoa sauti yake.[k] Na mbingu na dunia zitatikisika;[l] bali Yehova atakuwa kimbilio kwa watu wake,[m] na ngome kwa wana wa Israeli.[n] **17** Nanyi mtajua ya kwamba mimi ni Yehova Mungu wenu,[o] anayekaa katika Sayuni, mlima wangu mtakatifu.[a] Na Yerusalemu litakuwa mahali patakatifu;[b] wageni nao hawatapita tena kamwe kati yake.[c]

18 "Na itakuwa siku hiyo kwamba milima itatiririka divai tamu,[d] na vilima vitatiririka maziwa, na sakafu za vijito vya Yuda zitatiririka maji. Na katika nyumba ya Yehova bubujiko litatoka,[e] nalo litamwagilia maji bonde la mto la Mishita.[f] **19** Nayo Misri itakuwa mahame yenye ukiwa;[g] nayo Edomu itakuwa nyika ya mahame yenye ukiwa,[h] kwa sababu ya jeuri kwa wana wa Yuda, ambao walimwaga damu isiyo na hatia katika nchi yao.[i] **20** Bali Yuda, itakaliwa sikuzote,[j] na Yerusalemu kizazi baada ya kizazi.[k] **21** Na damu yao ambayo niliiona kuwa ina hatia nitaiona kuwa haina hatia;[l] Yehova naye atakuwa anakaa katika Sayuni."[m]

SURA 3

a Zb 103:20; 2Th 1:7; Ufu 19:14
b Yoe 3:2
c Zb 76:9; Zb 96:13
d Ufu 14:19
e Yer 51:33; Ufu 14:18
f Isa 63:3; Omb 1:15; Ufu 14:20
g Mwa 6:5; Isa 13:11
h Ufu 19:19
i Isa 34:2; Yoe 2:1; Sef 1:14
j Isa 13:10; Eze 32:7; Yoe 2:31; Mdo 2:20
k Yer 25:30; Amo 1:2
l Isa 13:13
m Zb 18:2; Zb 50:15
n Met 18:10
o Zb 9:16

Safu ya 2

a Oba 16; Zek 8:3
b Isa 4:3
c Isa 35:8; Isa 60:18; Nah 1:15; Zek 14:21; Ufu 21:27
d Amo 9:13; Zek 9:17
e Zb 46:4; Eze 47:1; Ufu 22:1
f Isa 41:19
g Isa 19:1
h Yer 49:17; Eze 25:13
i Amo 1:11; Oba 10
j Isa 33:20

k Zb 48:8; Isa 60:15; Amo 9:15; l Zb 103:10; Isa 4:4; Eze 36:25; Mik 7:19; m Zb 48:1; Isa 24:23; Mik 4:7.

AMOSI

1 Maneno ya Amosi, aliyekuwa kati ya wafugaji wa kondoo kutoka Tekoa,[a] ambayo aliona katika maono kuhusu Israeli[b] katika siku za Uzia[c] mfalme wa Yuda na katika siku za Yeroboamu[d] mwana wa Yoashi,[e] mfalme wa Israeli, miaka miwili kabla ya lile tetemeko la nchi.[f] **2** Naye akasema:

"Yehova—atanguruma kutoka Sayuni,[a] naye atatoa sauti yake kutoka Yerusalemu;[b] navyo viwanja vya malisho vya wachungaji vitaomboleza, na kilele cha Karmeli kitakauka."[c]

3 "Yehova amesema hivi, '"Kwa sababu ya maasi matatu ya Damasko,[d] na kwa sababu

SURA 1

a 2 Sa 14:2; 2 Nya. 11:6
b 2 Fal 17:13
c 2 Nya. 26:1; Isa 1:1; Hos 1:1
d 2 Fal 14:23; Amo 7:10
e 2 Fal 13:13
f Zek 14:5

Safu ya 2

a Yoe 3:16
b Yer 25:30
c 1 Sa 25:2; Isa 33:9; Nah 1:4

d Isa 7:8; Isa 8:4.

ya manne, sitaizuia, kwa sababu wamepura Gileadi[a] kwa vifaa vya kupuria vya chuma.
4 Nami nitapeleka moto[b] juu ya nyumba ya Hazaeli,[c] nao utaiteketeza minara ya makao ya Ben-hadadi.[d] **5** Nami nitavunja pingo la Damasko[e] na kumkatilia mbali mkaaji kutoka Bikath-aveni, na anayeshika fimbo ya enzi kutoka Bethedeni; na watu wa Siria wataenda Kiri[f] wakiwa wahamishwa," Yehova amesema.'

6 "Yehova amesema hivi, '"Kwa sababu ya maasi matatu ya Gaza,[g] na kwa sababu ya manne, sitaizuia, kwa sababu walilipeleka uhamishoni kundi zima la wahamishwa[h] ili kuwatia mkononi mwa Edomu.[i] **7** Nami nitapeleka moto kwenye ukuta wa Gaza,[j] nao utaiteketeza minara ya makao yake. **8** Nami nitakatilia mbali mkaaji kutoka Ashdodi,[k] na anayeshika fimbo ya enzi kutoka Ashkeloni;[l] nami nitageuza mkono wangu[m] juu ya Ekroni,[n] na mabaki ya Wafilisti yataangamia,"[o] Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema.'

9 "Yehova amesema hivi, 'Kwa sababu ya maasi matatu ya Tiro,[p] na kwa sababu ya manne, sitaizuia, kwa sababu ya kulitia mkononi mwa Edomu kundi zima la wahamishwa, na kwa sababu hawakukumbuka agano la ndugu.[q] **10** Nami nitapeleka moto kwenye ukuta wa Tiro, nao utaiteketeza minara ya makao yake.'[r]

11 "Yehova amesema hivi, 'Kwa sababu ya maasi matatu ya Edomu,[s] na kwa sababu ya manne, sitaizuia, kwa sababu alimfuatilia ndugu yake mwenyewe kwa upanga,[a] na kwa sababu aliharibu sifa zake mwenyewe za rehema,[b] na hasira yake huendelea kurarua milele, na ghadhabu yake—ameishika daima.[c] **12** Nami nitapeleka moto katika Temani,[d] nao utaiteketeza minara ya makao ya Bosra.'[e]

13 "Yehova amesema hivi, '"Kwa sababu ya maasi matatu ya wana wa Amoni,[f] na kwa sababu ya manne, sitaizuia,[g] kwa sababu waliwapasua wanawake wenye mimba wa Gileadi, kwa kusudi la kupanua eneo lao wenyewe.[h] **14** Nami nitawasha moto kwenye ukuta wa Raba,[i] nao utaiteketeza minara ya makao yake, pamoja na sauti ya king'ora siku ya pigano, pamoja na tufani siku ya upepo wa dhoruba.[j] **15** Na mfalme wao ataenda uhamishoni, yeye pamoja na wakuu wake,"[k] Yehova amesema.'

2 "Yehova amesema hivi, '"Kwa sababu ya maasi matatu ya Moabu,[l] na kwa sababu ya manne, sitaizuia, kwa kuwa aliteketeza mifupa ya mfalme wa Edomu ili kupata chokaa.[m] **2** Nami nitapeleka moto ndani ya Moabu, nao utaiteketeza minara ya makao ya Keriothi,[n] na Moabu atakufa kati ya kelele, na sauti ya king'ora, na sauti ya baragumu.[o] **3** Nami nitamkatilia mbali mwamuzi kutoka katikati yake, na wakuu wake wote nitawaua pamoja naye,"[p] Yehova amesema.'

4 "Yehova amesema hivi, 'Kwa sababu ya maasi matatu

SURA 1
a 2 Fal 8:12; 2 Fal 10:32; 2 Fal 10:33; 2 Fal 13:7
b Yer 49:27
c 1 Fal 19:15; 2 Fal 8:8
d 1 Fal 20:21
e Isa 7:8; Isa 17:1
f 2 Fal 16:9; Isa 22:6; Amo 9:7
g Eze 25:15
h 2 Nya. 21:17; 2 Nya. 28:18; Yoe 3:6
i Oba 11
j Yer 25:20; Yer 47:1; Zek 9:5
k Isa 20:1
l Yer 47:5
m Zab 81:14
n Sef 2:4; Zek 9:7
o Isa 14:29; Yer 47:4; Eze 25:16; Sef 2:5
p Eze 26:2
q Yoe 3:6
r Eze 26:12
s Isa 34:5; Yoe 3:19

Safu ya 2
a Eze 25:12
b Ayu 6:14
c 2 Nya. 28:17; Oba 10
d Mwa 36:11; Oba 9
e Mwa 36:33; Isa 34:6; Yer 49:13
f Eze 25:3; Sef 2:8
g Kum 23:3; 2 Nya. 20:1
h Amu 11:13; Yer 49:1; Eze 35:10
i Yer 49:2; Eze 25:5
j Zab 83:15
k Yer 27:3; Yer 49:3

SURA 2
l Yer 48:29; Eze 25:8; Sef 2:8
m Isa 33:12
n Yer 48:24
o Isa 15:1
p He 24:17; Isa 16:14; Yer 48:7

ya Yuda,[a] na kwa sababu ya
manne, sitaizuia, kwa saba-
bu wamekataa sheria ya Yeho-
va,[b] na kwa sababu hawaku-
shika masharti yake mwenye-
we; bali uwongo wao,[c] ambao
mababu zao walikuwa wame-
tembea ndani yake, uliende-
lea kuwapoteza.[d] **5** Nami ni-
tapeleka moto ndani ya Yuda,
nao utaiteketeza minara ya
makao ya Yerusalemu.'[e]

6 "Yehova amesema hivi,
'Kwa sababu ya maasi mata-
tu ya Israeli,[f] na kwa sababu
ya manne, sitaizuia, kwa saba-
bu waliuza mtu mwadilifu kwa
sababu tu ya fedha, na maski-
ni kwa bei ya pea moja ya via-
tu.[g] **7** Wanatamani sana ma-
vumbi ya dunia yaliyo kwenye
vichwa vya watu wa hali ya
chini;[h] nao huipotosha njia ya
watu wapole;[i] na mwanamume
na baba yake wamemwendea
msichana yuleyule,[j] kwa kusu-
di la kulitia unajisi jina langu
takatifu.[k] **8** Nao hujinyoo-
sha[l] kando ya kila madhaba-
hu[m] juu ya mavazi yaliyotwa-
liwa kama rehani; na divai ya
wale ambao wametozwa wao
huinywa katika nyumba ya mi-
ungu yao.'[n]

9 "'Lakini mimi, nilikuwa
nimemwangamiza Mwamori[o]
kwa sababu yao, ambaye ure-
fu wake ulikuwa kama urefu
wa mierezi, na ambaye aliku-
wa na nguvu kama miti miku-
bwa;[p] nami nikaangamiza ma-
tunda yake juu na mizizi yake
chini.[q] **10** Nami mwenyewe
niliwatoa ninyi kutoka nchi
ya Misri,[r] nami nikaendelea
kuwatembeza kupitia nyikani
miaka 40,[s] ili mwimiliki nchi
ya Mwamori.[a] **11** Nami nika-
endelea kuwasimamisha baa-
dhi ya wana wenu kuwa ma-
nabii[b] na baadhi ya wanaume
wenu vijana kuwa Wanadhiri.[c]
Je, kwa kweli haipaswi kuwa
hivyo, enyi wana wa Israeli?'
asema Yehova.

12 "'Lakini mliendelea ku-
wapa Wanadhiri divai wa-
nywe,[d] nanyi mkaweka amri
juu ya manabii, mkisema:
"Msitoe unabii."[e] **13** Tazama,
mimi nakifanya kile kilicho
chini yenu kiyumbe-yumbe,
kama vile linavyoyumba-yu-
mba gari la kukokotwa ambalo
limejazwa kabisa mafungu ya
nafaka iliyokatwa hivi karibu-
ni. **14** Na mahali pa kukimbi-
lia pataangamia kutoka kwa
yule aliye mwepesi,[f] wala haku-
na yeyote mwenye nguvu ata-
kayeimarisha nguvu zake, wala
hakuna mwanamume yeyote
mwenye nguvu ambaye atai-
ponya nafsi yake.[g] **15** Wala
yeyote anayetumia upinde ha-
tasimama, wala yeyote aliye
mwepesi kwa miguu yake ha-
taponyoka, wala mpandaji ye-
yote wa farasi hataiponya nafsi
yake.[h] **16** Na yule aliye na
moyo wenye nguvu kati ya wa-
naume wenye nguvu, ataki-
mbia akiwa uchi katika siku
ile,'[i] asema Yehova."

3 "Lisikieni neno hili amba-
lo Yehova amesema kuwa-
husu ninyi,[j] enyi wana wa Isra-
eli, kuhusu familia nzima ni-
liyoitoa katika nchi ya Misri,[k]
nikisema, **2** 'Mimi nimewa-
jua ninyi peke yenu[l] kati ya fa-
milia zote za nchi.[m] Hiyo ndi-

SURA 2
a 2 Fal 17:19; Yer 2:13; Yer 9:26
b Law 26:15; 2 Nya. 36:14; Ne 1:7; Dan 9:11
c Isa 28:15; Yer 16:19
d 2 Nya. 30:7; Yer 9:14
e 1 Sa 12:15; 1 Nya 28:9; 2 Nya. 36:19; Yer 17:27; Yer 37:8; Yer 52:13; Hos 8:14
f Kum 28:45; 2 Fal 17:7; Eze 23:5; Hos 4:1
g Kut 23:6; Eze 22:12; Yoe 3:3; Amo 5:11; Amo 8:6
h Amo 4:1
i Isa 10:2; Amo 5:12
j Law 18:8; Law 18:15; Eze 22:11; 1Ko 5:1
k Eze 36:20; Eze 43:8; Ro 2:24
l Kut 22:26; Kum 24:12; Eze 18:12
m Hos 8:11; Hos 10:1
n Amu 9:27
o He 21:24; Kum 2:31; Yos 24:8; Zab 135:11
p Isa 2:13
q Kum 2:32; Kum 2:33
r Kut 12:51; Zab 105:43; Mik 6:4
s He 14:34; Kum 2:7; Ne 9:21; Mdo 7:42

Safu ya 2
a Kum 1:20
b 1 Sa 3:20; 1 Fal 17:1; 1 Fal 19:19; 2 Nya. 36:15
c He 6:2; Amu 13:5; Omb 4:7
d He 6:3
e Isa 30:10; Yer 11:21; Amo 7:12; Mdo 4:18; 1Th 2:16
f Amo 9:1
g 2 Fal 25:5; Zab 33:16
h Isa 30:16
i Kum 28:25

SURA 3 j Isa 46:3; Hos 4:1; k Amo 2:10; l Kut 19:5; Kum 7:6; Zab 147:19; m Mwa 10:32; Yer 10:25.

yo sababu nitawatoza ninyi he-
sabu kwa sababu ya makosa
yenu yote.[a]
3 "'Je, watu wawili watate-
mbea pamoja isipokuwa wawe
wamekutana kwa mapatano?[b]
4 Je, simba atanguruma mwi-
tuni wakati hana mawindo yo-
yote?[c] Je, mwana-simba mwe-
nye manyoya shingoni ata-
toa sauti mafichoni mwake
ikiwa hakukamata chochote?
5 Je, ndege ataanguka nda-
ni ya mtego chini ikiwa haku-
na mnaso kwa ajili yake?[d] Je,
mtego huteguka udongoni iki-
wa haujakamata chochote ka-
mwe? **6** Je, baragumu ikipi-
gwa katika jiji, watu wenye-
we pia hawatetemeki?[e] Je, msi-
ba ukitokea katika jiji, Yehova
siye pia aliyetenda? **7** Kwa
maana Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova hatafanya lolote
isipokuwa awe amewafunulia
watumishi wake manabii ja-
mbo lake la siri.[f] **8** Kuna si-
mba ambaye amenguruma![g] Ni
nani hataogopa? Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova mwenye-
we amesema! Ni nani ambaye
hatatoa unabii?'[h]
9 "'Litangazeni kwenye mi-
nara ya makao katika Ashdodi
na juu ya minara ya makao ya
nchi ya Misri,[i] na kusema: "Ku-
sanyikeni pamoja juu ya mi-
lima ya Samaria,[j] mwone ma-
chafuko mengi yaliyo katikati
yake na visa vya upunjaji vili-
vyo ndani yake.[k] **10** Nao ha-
wajajua jinsi ya kufanya yali-
yo manyoofu,"[l] asema Yehova,
"wale wanaoweka jeuri[m] aki-
ba na uporaji katika minara ya
makao yao."'
11 "Kwa hiyo Bwana Mwe-
nye Enzi Kuu Yehova ame-
sema hivi, 'Kuna adui kuzu-
nguka nchi,[a] naye atazishusha
nguvu zako zikutoke, na mina-
ra ya makao yako itaporwa.'[b]
12 "Yehova amesema hivi,
'Kama vile mchungaji anavyo-
nyakua miguu miwili au ki-
pande cha sikio kutoka kati-
ka kinywa cha simba,[c] ndivyo
wana wa Israeli watakavyo-
nyakuliwa, wale wanaokaa ka-
tika Samaria kwenye kitanda
cha utukufu[d] na kwenye kita-
nda cha Damasko.'[e]
13 "'Sikieni na kutoa usha-
hidi[f] katika nyumba ya Ya-
kobo,' asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova, Mungu wa
majeshi. **14** 'Maana, siku ya-
ngu ya kutoza hesabu[g] kwa sa-
babu ya maasi ya Israeli juu
yake, mimi nitazitoza hesabu
pia madhabahu za Betheli;[h] na
pembe za madhabahu zitakati-
liwa mbali na kuanguka chini.[i]
15 Nami nitaiangusha nyu-
mba ya wakati wa majira ya ba-
ridi[j] kali pamoja na nyumba ya
wakati wa kiangazi.'[k]
"'Na nyumba za pembe za
tembo zitaangamia,[l] na nyu-
mba nyingi zitakwisha,'[m] ase-
ma Yehova."

4 "Lisikieni neno hili, ninyi
ng'ombe za Bashani,[n] mlio
juu ya mlima wa Samaria,[o] mna-
opunja watu wa hali ya chini,[p]
mnaoponda walio maskini,
mnaowaambia mabwana zenu,
'Leteni, tunywe!' **2** Bwana
Mwenye Enzi Kuu Yehova ame-
apa kwa utakatifu wake,[q] '"Ta-
zama! Kuna siku zinazokuja
juu yenu, naye atawainua ni-
nyi kwa kulabu za mchinjaji na

SURA 3
a Ayu 34:11; Yer 9:25; Eze 9:6; Dan 9:12; Hos 12:2; Amo 4:12; Ro 2:9
b Mwa 6:9; Mwa 17:1; 2Ko 6:14
c Zab 104:21; Isa 31:4
d Mhu 9:12
e Yer 4:5; Sef 1:16
f Mwa 6:13; Mwa 18:17; 1 Fal 22:23; 2 Fal 3:17; 2 Fal 22:20; Zab 25:14; Isa 42:9; Dan 9:22; Dan 11:2; Yn 15:15; Ufu 1:1
g Met 20:2; Met 30:30; Yer 4:7; Amo 1:2
h Yer 20:9; Amo 7:15; Mdo 4:20; Mdo 5:20
i Yer 46:14
j 2 Fal 17:23
k Isa 9:9; Hos 7:1; Amo 4:1
l Isa 26:10; Yer 4:22
m Sef 1:9

Safu ya 2
a 2 Fal 17:6; Isa 7:17
b Hos 11:6; Amo 6:8
c 1 Sa 17:34
d Isa 8:4
e Amo 6:4
f 2 Nya. 24:19; Eze 3:17
g Kut 32:34; Yer 9:25; Hos 4:9
h 1 Fal 12:33; 2 Fal 23:15; 2 Nya. 31:1; Hos 13:2
i 2 Nya. 34:7; Hos 10:2; Mik 1:6
j Yer 36:22
k Amu 3:20
l 1 Fal 22:39
m Isa 5:9; Amo 6:11

SURA 4
n Zab 22:12; Eze 39:18; Hos 4:16
o Amo 6:1
p Met 22:22; Hos 4:2; Mik 2:2; Mal 3:5; Yak 5:4
q Kut 15:11; Zab 89:35.

sehemu yenu ya mwisho kwa
ndoano.[a] **3** Nanyi mtakwenda
kupitia matundu,[b] kila mmoja
akienda mbele moja kwa moja;
nanyi mtatupwa nje kwenye
Harmoni," asema Yehova.'

4 "'Enyi watu, njooni Be-
theli, mfanye makosa.[c] Fanye-
ni makosa mara nyingi kati-
ka Gilgali,[d] na mlete dhabihu
zenu asubuhi; na sehemu zenu
za kumi katika siku ya tatu.[e]
5 Fukizeni dhabihu ya shu-
krani kutoka kwa kile kili-
chotiwa chachu,[f] na mtanga-
ze matoleo ya hiari;[g] litanga-
zeni, kwa maana hivyo ndivyo
mmependa, enyi wana wa Isra-
eli,'[h] asema Bwana Mwenye
Enzi Kuu Yehova.

6 "'Mimi pia, niliwapa ni-
nyi usafi wa meno[i] katika ma-
jiji yenu yote na upungufu
wa mkate katika mahali penu
pote;[j] lakini hamkurudi kwa-
ngu,'[k] asema Yehova.

7 "'Mimi pia, nilizuia mvua
isiwanyeshee ninyi kukiwa
kungali miezi mitatu kabla
ya mavuno;[l] nami nikainye-
sha katika jiji moja, lakini jiji
lingine sikuinyesha. Kuna se-
hemu moja ya shamba ambayo
ilinyeshewa, lakini sehemu ya
shamba ambayo sikuinyeshea
ilikauka.[m] **8** Na majiji mawili
au matatu yakayumba-yumba
kwenda kwenye jiji moja ili
kunywa maji,[n] nao hawakuto-
sheka;[o] lakini hamkurudi kwa-
ngu,' asema Yehova.

9 "'Niliwapiga ninyi kwa
kuunguza na kwa ukungu.[p]
Bustani zenu na mashamba
yenu ya matunda mliongeza,
lakini mitini yenu na mizeitu-
ni yenu ililiwa na kiwavi;[q] hata
hivyo hamkurudi kwangu,'[a]
asema Yehova.

10 "'Nilituma kati yenu ni-
nyi tauni kama ile ya Mi-
sri.[b] Niliwaua vijana wenu kwa
upanga,[c] pamoja na kuchukua
mateka farasi zenu.[d] Nami ni-
kaendelea kufanya harufu ya
kunuka ya kambi zenu ipande
hata kuingia puani mwenu;[e]
lakini hamkurudi kwangu,'[f]
asema Yehova.

11 "'Nilisababisha maanga-
mizi kati yenu, kama maanga-
mizi ya Mungu juu ya Sodo-
ma na Gomora.[g] Nanyi mkawa
kama kipande cha mti kilicho-
nyakuliwa kutoka motoni;[h] la-
kini hamkurudi kwangu,'[i] ase-
ma Yehova.

12 "Kwa hiyo hayo ndiyo ni-
takayokutendea, Ee Israeli.
Kwa sababu nitakutendea ma-
mbo hayo, jitayarishe kukuta-
na na Mungu wako,[j] Ee Israeli.
13 Kwa maana, tazama! Mfa-
nyizaji wa milima[k] na Muumba
wa upepo,[l] Yeye anayemwa-
mbia mtu wa udongo shughuli
zake za akilini,[m] Yeye anayefa-
nya mapambazuko kuwa giza,[n]
na Yeye anayetembea mahali
pa juu pa dunia,[o] Yehova Mu-
ngu wa majeshi ndilo jina
lake."[p]

5 "Lisikieni neno hili nina-
losema juu yenu kama wi-
mbo wa huzuni,[q] Ee nyumba
ya Israeli:

2 "Israeli, bikira,[r]
ameanguka;[s]
Hawezi kusimama tena.[t]
Ameachwa juu ya nchi
yake mwenyewe;
Hakuna
anayemsimamisha.[u]

SURA 4

a Hab 1:15
b 2 Fal 25:4
Eze 12:12
c 1 Fal 12:29
Eze 20:39
Hos 4:13
Amo 3:14
d Hos 4:15
Hos 9:15
Amo 5:5
e He 28:4
Kum 14:28
Kum 26:12
Hos 8:13
f Law 7:12
g Law 22:18
Kum 12:6
h Hos 9:1
i Kum 32:24
2 Fal 8:1
j Law 26:26
Kum 28:38
1 Fal 18:2
2 Fal 4:38
k 2 Nya. 28:22
Yer 3:7
Yer 5:3
l Kum 28:23
1 Fal 8:35
2 Nya. 7:13
Isa 5:6
m Yoe 1:20
n 1 Fal 18:5
Yer 14:3
o Yer 23:14
Hos 7:10
p Kum 28:22
1 Fal 8:37
Hag 2:17
q Kum 28:42

Safu ya 2

a Isa 42:24
Yer 5:3
b Kut 9:3
Kum 28:27
Kum 28:60
Zab 78:50
c Law 26:25
2 Fal 8:12
d 2 Fal 13:7
e Kum 28:26
f Yer 23:14
g Mwa 19:24
Yuda 7
h Zek 3:2
Yuda 23
i Eze 24:13
Hos 7:10
j Yer 17:10
Eze 18:30
Eze 22:31
Ebr 4:13
k Zab 65:6
Zab 95:4
Isa 40:12
l Zab 147:18
Yer 10:13
m Zab 139:2
Dan 2:28
n Kut 10:22
Kut 14:20
Isa 5:30
Yer 13:16
Amo 8:9
o Kum 32:13
Mik 1:3
p Isa 47:4
Yer 10:16

SURA 5

q Yer 7:29
Eze 19:1
Eze 27:2

r Yer 14:17; s Isa 3:8; t Isa 24:20; u Yer 2:28.

3 "Kwa maana Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi, 'Jiji lililokuwa likitoka nje likiwa na elfu moja litaachwa na mia; na lile lililokuwa likitoka nje likiwa na mia moja litaachwa na kumi, kwa nyumba ya Israeli.'[a]

4 "Kwa maana Yehova ameiambia hivi nyumba ya Israeli, 'Nitafuteni mimi,[b] mwendelee kuishi.[c] **5** Wala msitafute Betheli,[d] wala msiende Gilgali,[e] wala msivuke Beersheba;[f] kwa sababu Gilgali litakwenda uhamishoni;[g] Betheli nalo litakuwa kitu cha uchawi.[h] **6** Mtafuteni Yehova, Ee nyumba ya Yosefu,[i] mwendelee kuishi,[j] ili asitende kama vile moto,[k] nao usije ukateketeza, na Betheli lisikose mtu wa kuuzima,[l] **7** enyi mnaoigeuza haki kuwa pakanga tupu,[m] ninyi ambao mmeutupa chini uadilifu.[n] **8** Mtengenezaji wa kundi-nyota la Kima[o] na kundi-nyota[p] la Kesili,[q] na Yeye ambaye anageuza kivuli kizito[r] kiwe asubuhi, na Yeye ambaye amefanya mchana uwe na giza kama usiku,[s] Yeye ambaye anaita maji ya bahari, ili ayamwage kwenye uso wa dunia[t]—Yehova ndilo jina lake;[u] **9** yeye ambaye anasababisha uporaji uje ghafula juu ya mtu mwenye nguvu, ili uporaji uje hata juu ya mahali penye ngome.

10 "'Katika lango wao wamemchukia mwenye kukaripia,[v] nao humchukia msemaji wa mambo makamilifu.[w] **11** Basi, kwa sababu mnamtoza mtu wa hali ya chini kodi ya shamba,[x] nanyi mnaendelea kuchukua kutoka kwake ushuru wa nafaka; mmejenga nyumba za mawe yaliyochongwa,[a] lakini hamtaendelea kukaa ndani yake; nanyi mmepanda mashamba ya mizabibu yenye kupendeza, lakini hamtaendelea kunywa divai yake.[b] **12** Kwa maana nimejua hesabu za maasi[c] yenu na jinsi dhambi zenu zilivyo kubwa,[d] enyi mnaomwonyesha mtu mwadilifu uadui,[e] ninyi mnaochukua pesa za hongo,[f] na ambao mmewafukuza watu maskini[g] langoni.[h] **13** Basi yeye aliye na ufahamu atakaa kimya wakati huo, kwa maana utakuwa wakati wenye taabu.[i]

14 "'Tafuteni yaliyo mema, wala si yaliyo mabaya,[j] kusudi mwendelee kuishi;[k] ndipo Yehova Mungu wa majeshi apate kuwa pamoja nanyi, kama vile ambavyo mmesema.[l] **15** Chukieni yaliyo mabaya, pendeni yaliyo mema,[m] na mwipatie haki nafasi langoni.[n] Huenda ikawa Yehova Mungu wa majeshi atawapa kibali[o] mabaki ya Yosefu.'[p]

16 "Basi Yehova aliye Yehova Mungu wa majeshi amesema hivi, 'Kutakuwako maombolezo katika viwanja vyote vya watu wote,[q] na katika barabara zote watu watakuwa wakisema: "Ah! Ah!" Nao watamwita mkulima aje kuomboleza,[r] na kuwaita wale wenye uzoefu wa maombolezo waje kulia.'[s] **17** 'Na kutakuwako maombolezo katika mashamba yote ya mizabibu;[t] kwa maana nitapita katikati yako,'[u] Yehova amesema.

SURA 5

a Kum 4:27
Kum 28:62
Isa 10:22
b 2 Nya. 15:2
Isa 55:6
Yer 29:12
c Zab 69:32
Met 4:4
Isa 55:3
d 1 Fal 12:29
Amo 4:4
e Hos 4:15
f Amo 8:14
g 2 Fal 17:6
Hos 9:15
h Isa 1:13
i Zek 10:6
j Eze 33:11
k Ebr 12:29
l Eze 20:47
m Amo 6:12
n Eze 3:20
Eze 18:24
o Ayu 9:9
p Ayu 38:31
q Isa 13:10
r Ayu 12:22
s Kut 10:21
t Ayu 36:27
Mhu 1:7
u Zab 83:18
Amo 4:13
v 1 Fal 18:17
Met 13:19
Isa 29:21
w 1 Fal 22:8
1Pe 3:16
x Mik 2:2

Safu ya 2

a Isa 9:10
Sef 1:13
b Kum 28:30
Hag 1:6
c Kum 31:21
Yer 29:23
d 2 Fal 17:7
e Zab 37:12
Amo 2:6
f 1 Sa 12:3
g Kum 15:7
Isa 29:21
Eze 22:12
Amo 2:7
Yak 2:6
h Met 22:22
Isa 10:2
i Mik 2:3
j Met 11:27
Isa 1:16
Mik 6:8
Ro 2:7
k Law 18:5
Kum 30:20
Zab 69:32
Ro 10:5
l 2 Nya. 15:2
Mik 3:11
Mik 7:20
m Zab 34:14
Zab 97:10
Ro 12:9
3Yh 11
n 2 Nya. 19:6
Amo 5:24
o Kut 32:30
Zab 62:12
Sef 2:3
p Yer 31:7
Zek 10:6
q Isa 22:12
Yer 9:10
r Yoe 1:11
s Yer 9:17

t Isa 16:10; Yer 48:33; Hos 9:2; u Kut 12:12; Nah 1:12.

18 "'Ole wao wanaoitamani
siku ya Yehova![a] Basi, siku ya
Yehova itamaanisha nini kwe-
nu?[b] Itakuwa giza, wala si nuru,[c]
19 kama vile tu mtu anavyo-
mkimbia simba, kisha dubu
anakutana naye; na kama vile
alivyoingia ndani ya nyumba
akauegemeza mkono wake
ukutani, naye nyoka akamu-
uma.[d] **20** Je, siku ya Yehova
haitakuwa giza, wala si nuru;
na je, haitakuwa na weusi,
wala si mwangaza?[e] **21** Ni-
mechukia, nimezikataa she-
rehe zenu,[f] wala sitafurahia
harufu ya makusanyiko yenu
makuu.[g] **22** Lakini ninyi
mkinitolea matoleo mazima
ya kuteketezwa,[h] hata kati-
ka matoleo yenu ya zawadi
sitapata furaha,[i] wala sita-
tazama dhabihu zenu za ushi-
rika za vinono.[j] **23** Ondoe-
ni kutoka kwangu mchafuko
wa nyimbo zenu; wala sauti
tamu ya vinanda vyenu sita-
ki kusikia.[k] **24** Na haki iti-
ririke kama maji,[l] na uadili-
fu kama mto unaotiririka daima.[m]
25 Je, mlinisogezea ka-
ribu dhabihu na matoleo ya
zawadi nyikani miaka 40, Ee
nyumba ya Israeli?[n] **26** Na-
nyi mtamchukua Sakuthi mfa-
lme wenu[o] na Kaiwani, sana-
mu zenu, nyota ya mungu
wenu, ambaye mlijifanyia ni-
nyi wenyewe.[p] **27** Nami nita-
wafanya mwende uhamisho-
ni ng'ambo ya Damasko,'[q]
yeye ambaye jina lake ni Ye-
hova Mungu wa majeshi, ame-
sema."[r]

6 "Ole wao wanaostarehe[s]
katika Sayuni na wale wa-
naotegemea mlima wa Sama-
ria! Hao ndio wale walio ma-

SURA 5

a Isa 5:19
Yer 17:15
Mal 3:2
b Yer 30:7
Yoe 1:15
Amo 4:12
c Sef 1:15
d 1 Fal 20:30
Isa 24:17
Isa 24:18
Yer 15:2
e Eze 34:12
Ufu 16:10
f Met 15:8
Met 21:27
Isa 1:11
Yer 6:20
g Mwa 8:21
Law 26:31
h Zab 50:8
Isa 66:3
Hos 6:6
i Mwa 4:5
Law 7:12
j Isa 1:11
k Met 28:9
Amo 6:5
Amo 8:10
l Met 21:3
Mik 6:8
Ebr 13:16
m Ro 14:17
n Yos 24:14
Eze 20:8
Mdo 7:42
o Law 20:2
p Kut 20:4
Zab 115:8
Mdo 7:43
q 2 Fal 15:29
2 Fal 17:6
r Amo 4:13

SURA 6

s 1 Fal 22:39
Amo 3:15

Safu ya 2

a He 34:8
2 Fal 14:28
b 2 Nya. 26:6
c Isa 10:10
Nah 3:8
d Zab 10:13
Mhu 8:11
Isa 56:12
Eze 12:27
2Pe 3:4
e Amo 5:12
f 1 Fal 22:39
g Isa 22:13
h Isa 5:12
i 2 Nya. 7:6
2 Nya. 29:25
j Isa 5:11
k Mt 26:7
Yn 12:3
l 2 Fal 15:29
2 Fal 17:6
m Kum 28:41
Amo 5:5
n Yer 51:14
Amo 4:2
Ebr 6:13
o Met 16:18
Eze 33:28
Hos 5:5
p Omb 2:5
q Mik 1:6

shuhuri wa sehemu kuu ya
mataifa, na nyumba ya Isra-
eli imewajia. **2** Shikeni njia
mpaka Kalne, mkaone; na ku-
toka hapo endeni mpaka Ha-
mathi[a] jiji lililo na hesabu ku-
bwa ya watu, na mshuke mpa-
ka Gathi[b] la Wafilisti. Je, hayo
ni bora kuliko falme hizi, au je,
eneo lao ni kubwa kuliko eneo
lenu?[c] **3** Je, mnaiondoa akili-
ni mwenu ile siku yenye msi-
ba,[d] na je, mnaleta karibu ma-
kao ya jeuri?[e] **4** Ninyi watu
mnaojilaza katika vitanda vya
pembe za tembo[f] na kujita-
ndaza katika vitanda vyao, na
mnaokula kondoo-dume kati
ya kundi na ng'ombe-dume wa-
changa kutoka kati ya ndama
waliononeshwa;[g] **5** ambao
mnatunga kulingana na sauti
ya kinanda,[h] ambao, kama Da-
udi, mmejitengenezea vyombo
vya nyimbo;[i] **6** ambao mna-
kunywa kwa mabakuli ya di-
vai,[j] na ambao mnatia mafu-
ta kwa kutumia mafuta yenu
yaliyo bora kabisa,[k] na ambao
hamkuwa wagonjwa kutokana
na msiba wa Yosefu.[l]

7 "Basi sasa wataenda uha-
mishoni wakiwa mbele ya wale
wanaoenda uhamishoni,[m] na
karamu za kupindukia za wale
wanaojitandaza zitaondoka.

8 "'Bwana Mwenye Enzi
Kuu Yehova ameapa kwa na-
fsi yake mwenyewe,'[n] asema
Yehova Mungu wa majeshi,
'"Mimi ninachukia kiburi cha
Yakobo,[o] na minara ya makao
yake nimeichukia,[p] nami nita-
litoa hilo jiji na vitu vyote vi-
navyolijaza.[q] **9** Na itakuwa
kwamba wanaume kumi waki-
baki katika nyumba moja, wao

pia watakufa.[a] **10** Na ndugu ya baba yake atawachukua mmoja mmoja, naye atawachoma moto mmoja mmoja, ili kuiondoa mifupa ndani ya nyumba.[b] Naye atamwambia yeyote yule aliye katika sehemu za ndani kabisa za nyumba, 'Je, bado una wengine zaidi?' Naye atalazimika kusema, 'Hamna mtu!' Naye atalazimika kusema, 'Nyamaza kimya! Kwa maana huu si wakati wa kutaja kwa vyovyote jina la Yehova.'"[c]

11 "'Kwa maana ni Yehova anayeamuru,[d] naye ataipiga ile nyumba kubwa kwa kuifanya kuwa mabomoko na ile nyumba ndogo kwa kuifanya kuwa magofu.[e]

12 "'Je, farasi watakimbia juu ya mwamba, au je, mtu atalima hapo kwa kutumia ng'ombe? Kwa maana ninyi mmeigeuza haki iwe mmea wenye sumu,[f] na kuyageuza matunda ya uadilifu yawe pakanga, **13** ninyi mnaoshangilia jambo ambalo halipo;[g] ambao mnasema: "Je, hatukujitwalia pembe kwa nguvu zetu wenyewe?"[h] **14** Tazama! Mimi ninasimamisha taifa juu yenu,[i] Ee nyumba ya Israeli,' asema Yehova Mungu wa majeshi, 'nao watawakandamiza ninyi kutoka maingilio ya Hamathi[j] mpaka kwenye bonde la mto la Araba.'"

7 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova alinifanya nione, na, tazama! alikuwa akifanyiza kundi la nzige mwanzoni mwa kuota kwa mimea iliyopandwa baadaye.[k] Na, tazama! ilikuwa mimea iliyopandwa baadaye baada ya majani yaliyofyekwa ya mfalme. **2** Na ikawa kwamba lilipomaliza kula kabisa majani ya nchi, nikasema: "Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, tafadhali samehe.[a] Ni nani atakayesimama katika Yakobo? Maana yeye ni mdogo!"[b]

3 Yehova akajuta juu ya jambo hilo.[c] "Hilo halitatokea," Yehova akasema.

4 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova alinifanya nione, na, tazama! Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova alikuwa anaita mashindano kupitia kwa moto;[d] nao ukateketeza kabisa kilindi kikubwa cha maji na kuteketeza kabisa ile sehemu ya shamba. **5** Nami nikasema: "Ee Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, tafadhali zuilia.[e] Ni nani atakayesimama katika Yakobo? Maana yeye ni mdogo!"[f]

6 Yehova akajuta juu ya jambo hilo.[g] "Hilo pia halitatokea," Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova akasema.

7 Hili ndilo alilonifanya nione, na, tazama! Yehova alikuwa juu ya ukuta uliotengenezwa kwa timazi,[h] na timazi ilikuwa mkononi mwake. **8** Ndipo Yehova akaniambia: "Unaona nini, Amosi?" Basi nikasema: "Timazi." Yehova akaendelea kusema: "Tazama, naweka timazi katikati ya watu wangu Israeli.[i] Nami sitawasamehe zaidi tena.[j] **9** Na mahali pa juu pa Isaka[k] patafanywa kuwa ukiwa, na patakatifu[l] pa Israeli pataharibiwa;[m] nami nitasimama kuipiga nyumba ya Yeroboamu kwa upanga."[n]

SURA 6
a Zab 109:13
b 1 Sa 31:12
c 2 Fal 6:33
d Isa 10:5
Isa 55:11
e 2 Fal 25:9
Amo 3:15
f 1 Fal 21:13
Zab 94:20
Isa 59:13
Hos 10:4
Amo 5:7
g Isa 44:9
h Kum 8:17
Zab 75:5
Dan 4:30
i Kum 28:49
2 Fal 15:29
2 Fal 17:6
Isa 7:20
Isa 8:4
Isa 10:5
Hos 10:6
j He 34:8
1 Fal 8:65

SURA 7
k Yoe 1:4
Yoe 2:25

Safu ya 2
a Zab 130:4
Yer 14:7
Dan 9:19
b Isa 37:4
Yer 42:2
c Kum 32:36
Zab 106:45
Hos 11:8
Yon 3:10
Yak 5:16
d Yer 4:4
e Kut 32:11
f Isa 1:9
g Kut 32:14
h Zek 4:10
i Omb 2:8
j Yer 15:6
Eze 7:2
Amo 8:2
k 1 Fal 12:32
Hos 10:8
l 1 Fal 12:31
m Amo 5:5
Amo 8:14
n 2 Fal 15:10
Hos 13:16

10 Naye Amazia kuhani wa Betheli[a] akapeleka habari kwa Yeroboamu[b] mfalme wa Israeli, akisema: "Amosi amepanga hila juu yako ndani ya nyumba ya Israeli.[c] Nchi haiwezi kuvumilia maneno yake yote.[d] **11** Kwa maana Amosi amesema hivi, 'Kwa upanga Yeroboamu atakufa; naye Israeli bila shaka ataenda uhamishoni kutoka katika nchi yake mwenyewe.'"[e]

12 Kisha Amazia akamwambia Amosi: "Ewe mwonaji,[f] nenda, kimbia uende zako kwenye nchi ya Yuda, ukale mkate huko, na huko unaweza kutoa unabii. **13** Lakini usiendelee tena kutoa unabii katika Betheli,[g] kwa maana ni mahali patakatifu pa mfalme[h] napo ni nyumba ya ufalme."

14 Ndipo Amosi akajibu na kumwambia Amazia: "Mimi sikuwa nabii, wala sikuwa mwana wa nabii,[i] bali nilikuwa mchungaji[j] na mminyaji wa tini za mikuyu. **15** Naye Yehova akanichukua nisifuatane na kundi tena, na Yehova akaendelea kuniambia, 'Nenda, watolee unabii watu wangu Israeli.'[k] **16** Basi sasa lisikie neno la Yehova, 'Je, unasema: "Usitoe unabii juu ya Israeli,[l] wala usiache neno lolote lianguke[m] juu ya nyumba ya Isaka"? **17** Basi Yehova amesema hivi: "Kwa habari ya mke wako, atakuwa kahaba jijini.[n] Nao wana na binti zako wataanguka kwa upanga. Nayo nchi yako itagawanywa kwa kamba ya kupimia. Na wewe mwenyewe utakufa katika nchi isiyo safi;[o] naye Israeli, bila shaka ataenda uhamishoni kutoka katika nchi yake mwenyewe."'"[p]

SURA 7
a 1 Fal 12:32; 1 Fal 13:33
b 2 Fal 14:23
c Yer 26:8
d Yer 18:18; Lu 23:2
e Amo 5:5; Amo 6:7
f Isa 30:10
g Amo 2:12; Mdo 4:17; Mdo 5:28
h 1 Fal 12:29; 1 Fal 12:32; 1 Fal 13:1
i 1 Fal 20:35; 2 Fal 4:38
j Amo 1:1
k Yer 1:7; Eze 2:3; 2Pe 1:21
l Yer 11:21; Amo 7:13
m Kum 32:2; Mik 2:6
n Omb 5:11
o 2 Fal 17:6
p Law 26:33; Yer 36:31

Safu ya 2

SURA 8
a Yer 24:1
b Yer 1:11
c Yer 24:8
d Omb 4:18; Eze 7:2
e Amo 4:12; Amo 7:8
f Hos 10:5; Yoe 1:13; Amo 5:23
g Yer 9:21; Amo 6:10
h Zab 37:14; Zab 140:12; Met 30:14
i Zab 14:4; Amo 2:6
j He 10:10
k Ne 10:31
l Kut 20:8; Ne 13:15
m Law 19:36; Mik 6:10
n Met 11:1; Met 20:23; Hos 12:7
o Law 25:39; Amo 2:6
p Kum 33:26; Zab 47:4; Zab 68:34
q Yer 17:1; Hos 8:13; Nah 1:3
r Isa 5:25
s Hos 4:3
t Amo 9:5
u Yer 15:9; Mik 3:6; Mt 24:29

8 Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova alinifanya nione, na, tazama! kulikuwako kikapu cha matunda ya wakati wa kiangazi.[a] **2** Kisha akasema: "Unaona nini,[b] Amosi?" Basi nikasema: "Kikapu cha matunda ya wakati wa kiangazi."[c] Na Yehova akaendelea kuniambia: "Mwisho umewafikia watu wangu Israeli.[d] Nami sitawasamehe zaidi tena.[e] **3** 'Na nyimbo za hekalu zitakuwa mayowe siku hiyo,'[f] asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. 'Kutakuwako mizoga mingi.[g] Kila mahali mtu fulani ataitupa—kimya!'

4 "Sikieni hili, ninyi mnaouma maskini,[h] ili kuwakomesha wapole wa dunia,[i] **5** mkisema, 'Mwezi mpya utapita wakati gani,[j] tukauze nafaka?[k] Pia sabato,[l] tukauze nafaka; ili kuifanya efa kuwa ndogo[m] na kuifanya shekeli kuwa kubwa na kuipotosha mizani ya udanganyifu;[n] **6** ili tununue watu wa hali ya chini kwa fedha tu na maskini kwa bei ya pea moja ya viatu, na ili tuuze takataka tupu ya nafaka?'[o]

7 "Yehova ameapa kwa Ukuu wa Yakobo,[p] 'Kamwe sitazisahau kazi zao zote.[q] **8** Je, haitakuwa kwa sababu hii kwamba nchi itafadhaika,[r] na kila mkaaji ndani yake ataomboleza;[s] nayo yote, itainuka kama tu Nile na kurushwarushwa na kuzama kama mto Nile wa Misri?'[t]

9 "'Na itakuwa katika siku hiyo,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'kwamba nitalifanya jua lishuke katikati ya mchana,[u] nami nitaile-

tea nchi giza siku ya mwangaza. **10** Nami nitazigeuza sherehe zenu ziwe maombolezo[a] na nyimbo zenu zote ziwe nyimbo za huzuni. Nitatia nguo za magunia juu ya viuno vyote na juu ya kila kichwa nitatia upara.[b] Nami nitafanya hali iwe kama kuombolezea mwana wa pekee,[c] na matokeo yake ya mwisho kama siku yenye uchungu.'

11 "'Tazama! Siku zinakuja,' asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova, 'nami nitaleta njaa katika nchi, wala si njaa ya mkate, nami nitaleta kiu, wala si kiu ya maji, bali ya kuyasikia maneno ya Yehova.[d] **12** Nao wataenda wakiyumba-yumba kutoka bahari mpaka bahari, kutoka kaskazini hata mashariki. Watazidi kwenda huku na huku wakitafuta neno la Yehova, lakini hawatalipata.[e] **13** Katika siku hiyo mabikira wenye kupendeza watazimia, pia vijana, kwa sababu ya kiu;[f] **14** wale wanaoapa kwa hatia ya Samaria,[g] na ambao husema: "Kama anavyoishi mungu wako, Ee Dani!"[h] na, "Kama inavyoishi njia ya Beer-sheba!"[i] Nao watanguka, wala hawatasimama tena.' "[j]

9 Nilimwona Yehova akiwa juu ya madhabahu,[k] naye akasema: "Kipige kichwa cha nguzo, ili vizingiti vitikisike. Na uvikate vyote kichwani.[l] Na sehemu yao ya mwisho nitaua kwa upanga. Hakuna yeyote kati yao anayekimbia atakayefanikiwa kukimbia, na hakuna yeyote kati yao anayeponyoka ambaye atafaniki-

SURA 8

a Hos 2:11
b Eze 7:18
c Yer 6:26
Lu 7:12
d 1 Sa 3:1
Zab 74:9
Eze 7:26
Mt 4:4
e Met 1:28
f Omb 2:19
g Yos 23:7
1 Fal 12:30
Hos 8:5
Hos 10:5
h 1 Fal 12:29
i Amo 5:5
j 2 Fal 18:11
Hos 13:16

SURA 9

k Isa 6:1
Eze 1:28
l Zab 68:21
Hab 3:13

Safu ya 2

a Isa 24:18
Isa 30:16
Amo 2:14
b Zab 139:8
Met 15:11
c Ayu 20:6
Yer 49:16
Yer 51:53
Oba 4
d Ayu 34:22
Zab 139:7
Yer 23:24
e Zab 139:9
f Law 26:33
Kum 28:65
Eze 5:12
g Law 17:10
Kum 28:63
Yer 44:11
1Pe 3:12
h Zab 46:6
Mik 1:4
i Hos 4:3
j Amo 8:8
k Zab 102:19
l Isa 45:18
m Ayu 36:27
Zab 135:7
n Zab 147:8
Amo 5:8
o Kut 3:15
Yer 31:35
Amo 4:13
p Kut 12:51
Hos 12:13
Amo 2:10
q Yer 47:4
r 2 Fal 16:9
Isa 22:6
Amo 1:5
s Zab 11:4
Met 5:21
Met 15:3

wa kutoroka.[a] **2** Wakichimba chini kuingia katika Kaburi,* toka humo mkono wangu mwenyewe utawachukua;[b] nao wakienda juu mbinguni, toka huko nitawashusha chini.[c] **3** Nao wakijificha katika kilele cha Karmeli, nitawatafuta kwa uangalifu na kuwachukua kutoka huko.[d] Na wakijificha kwenye sakafu ya bahari kutoka mbele za macho yangu,[e] huko chini nitamwamuru nyoka, naye atawauma. **4** Nao wakienda utekwani mbele ya adui zao, kutoka huko nitaamuru upanga, nao utawaua;[f] nami nitaweka macho yangu juu yao kwa mabaya, wala si kwa mema.[g] **5** Naye Bwana Mwenye Enzi Kuu, Yehova wa majeshi, Yeye ndiye anayeigusa nchi, ikayeyuka;[h] na wakaaji wote ndani yake wataomboleza.[i] Nayo yote itainuka kama Nile, na kuzama kama mto Nile wa Misri.[j]

6 "'Yeye anayejenga ngazi zake huko mbinguni,[k] na jengo lake juu ya dunia ambayo ameiwekea msingi;[l] yeye anayeyaita maji ya bahari,[m] ili ayamwage juu ya uso wa dunia[n]—Yehova ndilo jina lake.'[o]

7 "'Je, ninyi si kama wana wa Wakushi kwangu, enyi wana wa Israeli?' asema Yehova. 'Je, sikuleta Israeli kutoka nchi ya Misri,[p] na Wafilisti[q] kutoka Krete, na Siria kutoka Kiri?'[r]

8 "'Tazama! Macho ya Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova yako juu ya ufalme wenye dhambi,[s] naye atauangamiza kutoka

Amo 9:2* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

juu ya uso wa nchi.[a] Hata hivyo, sitaiangamiza kabisa nyumba ya Yakobo,"[b] asema Yehova. **9** 'Kwa maana, tazama! Ninaamuru, nami nitaipepeta nyumba ya Israeli katika mataifa yote,[c] kama vile mtu anavyopepeta kichujio, lisianguke chini jiwe la mviringo hata moja. **10** Kwa upanga watakufa—watenda-dhambi wote katika watu wangu,[d] wale wanaosema: "Taabu hiyo haitakuja karibu wala kutufikia sisi."'[e]

11 "'Katika siku hiyo nitakisimamisha[f] kibanda[g] cha Daudi ambacho kimeanguka,[h] nami nitayarekebisha matundu yao. Na mabomoko yake nitayasimamisha, nami nitakijenga kama katika siku za kale,[i] **12** ili kwamba wamiliki mabaki ya Edomu,[j] na mataifa yote ambayo juu yao jina langu limeitwa,'[a] asema Yehova, anayefanya hayo.

13 "'Tazama! Siku zinakuja,' asema Yehova, 'na anayelima atampita anayevuna,[b] na anayekanyaga zabibu atampita anayechukua mbegu;[c] na milima itatiririka divai tamu,[d] na vilima vyote vitayeyuka.[e] **14** Nami nitakusanya na kurudisha mateka wa watu wangu Israeli,[f] nao watajenga majiji yaliyofanywa ukiwa na kukaa ndani yake,[g] watapanda mashamba ya mizabibu na kunywa divai yake, watafanyiza bustani na kula matunda yake.'[h]

15 "'Nami nitawapanda juu ya nchi yao, wala hawatang'olewa tena kutoka katika nchi yao ambayo nimewapa,'[i] Yehova Mungu wako amesema."

SURA 9

a 1 Fal 13:34; 2 Fal 18:11
b Yer 30:11
c Law 26:33; Kum 28:64
d 2 Fal 18:12; Eze 20:38; Nah 1:3
e Zab 10:13; 2Pe 3:4
f Isa 9:6; Isa 11:1; Yer 23:5; Eze 17:24; Eze 37:24; Zek 12:8; Lu 1:31
g Isa 16:5
h Eze 21:27; Mdo 15:16
i 2 Sa 7:11; Zab 89:36
j He 24:18; Isa 11:14; Oba 19

Safu ya 2

a Mdo 15:17
b Law 26:5; Eze 36:35
c Hos 2:22
d Yoe 3:18
e Isa 35:1; Isa 55:12
f Ezr 3:1; Yer 30:3; Eze 39:25
g Isa 61:4; Isa 65:21; Eze 36:33

h Isa 62:8; Yer 30:10; Eze 28:26; Mik 4:4; i Isa 60:21; Yer 24:6; Eze 34:28; Eze 37:25; Yoe 3:20.

OBADIA

1 Maono ya Obadia:

Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova amesema hivi kuhusu Edomu:[a] "Kuna habari ambayo tumesikia kutoka kwa Yehova, na kuna mjumbe ambaye ametumwa kati ya mataifa, 'Simameni, na tusimame tupigane naye.'"[b]

2 "Tazama! Nimekufanya mdogo kati ya mataifa.[c] Unadharauliwa sana.[d] **3** Kimbelembele cha moyo wako ndicho kimekudanganya,[e] wewe unayekaa katika makimbilio ya mwamba,[f] kwenye kilele ambapo yeye hukaa, akisema moyoni mwake, 'Ni nani atakayenishusha chini duniani?' **4** Ukipafanya mahali pako pawe juu kama tai, au ikiwa kiota chako kingewekwa kati ya nyota, ningekushusha chini kutoka hapo,"[a] asema Yehova.

5 "Ikiwa wezi ndio wangekuja kwako, ikiwa waporaji wangekuja wakati wa usiku, ungenyamazishwa kwa kadiri gani?[b] Je, hawangeiba kadiri wanavyotaka? Au ikiwa wakusanya-zabibu ndio wangekuja kwako, je, hawange-

a Isa 21:11; Eze 25:12; Yoe 3:19; Amo 1:11
b Yer 49:14; Oba 15; Mal 1:4
c Yer 49:15
d Yer 49:8
e Met 16:18; Yer 49:16; Mal 1:4
f 2Nya 25:12

Safu ya 2

a Yer 49:16; Amo 9:2
b Yer 49:9

acha masalio fulani?[a] **6** Lo!
jinsi ambavyo walio wa
Esau wametafutwa![b] Jinsi ha-
zina zake zilizofichwa zime-
tafutwa! **7** Wamekufukuza
hadi mpakani. Watu walewa-
le walio katika agano pamo-
ja nawe wamekudanganya[c]
wote. Watu walio na amani
pamoja nawe wamekushinda.[d]
Wale wanaokula chakula pa-
moja nawe wataweka wavu
chini yako kama mtu asiye na
utambuzi.[e] **8** Je, haitakuwa
katika siku hiyo?" asema Ye-
hova.

"Nami nitawaangamiza we-
nye hekima kutoka Edomu,[f]
na utambuzi kutoka eneo le-
nye milima la Esau. **9** Na
wanaume wako wenye ngu-
vu wataingiwa na woga,[g] Ee
Temani,[h] kwa kuwa kila mmo-
ja atakatiliwa mbali[i] kutoka
katika eneo lenye milima la
Esau, kwa sababu ya kuuawa.[j]
10 Kwa sababu ya jeuri uliyo-
mtendea ndugu yako Yakobo,[k]
aibu itakufunika,[l] nawe utaka-
tiliwa mbali mpaka wakati
usio na kipimo.[m] **11** Siku uli-
yosimama kando, siku amba-
yo wageni walichukua jeshi
lake na kulipeleka utekwa-
ni[n] na wageni kabisa walipoi-
ngia katika lango lake,[o] waka-
piga kura[p] juu ya Yerusalemu,
wewe pia ulikuwa kama mmo-
ja wao.

12 "Nawe hupaswi kutaza-
ma tukio katika siku ya ndu-
gu yako,[q] katika siku ya maafa
yake; wala kushangilia juu ya
wana wa Yuda katika siku ya
kuangamia kwao;[r] wala usise-
me makuu katika siku ya taa-
bu yao. **13** Hupaswi kuja ka-

a Kum 24:21
Isa 17:6
b Yer 49:10
c Yer 27:6
Omb 1:19
Eze 23:22
d Yer 38:22
e Yer 49:7
f Zb 33:10
1Ko 3:19
g Zb 76:7
Yer 49:22
h Mwa 36:11
Eze 25:13
Amo 1:12
i Isa 34:6
j Isa 34:5
k Mwa 27:42
Hes 20:20
Zb 83:5
Zb 137:7
Yoe 3:19
Amo 1:11
l Yer 49:13
m Mal 1:3
Mal 1:4
n 2Fa 24:10
2Fa 25:5
Yer 52:28
o 2Fa 25:4
p Yoe 3:3
q Mik 4:11
r Met 17:5
Met 24:17
Omb 4:21

Safu ya 2

a Zek 1:15
b Zb 137:7
Eze 25:12
c Zb 83:4
Amo 1:11
d Yer 30:7
e Yer 9:25
Yer 25:32
Yer 49:12
Yoe 3:14
Mik 5:15
2Pe 3:10
f Eze 35:15
Mt 7:2
g Yer 30:23
2Th 1:6
Yak 2:13
h Yer 25:17
Yer 49:12
i Yoe 2:32
j Isa 4:3
Zek 8:3
k Isa 14:2
Eze 35:10
Amo 9:12
l Isa 10:17
Zek 12:6
m Isa 5:24
n Yer 49:18
Eze 35:15
Oba 9
o Isa 11:14
Amo 9:12
p Amo 1:8
q Yer 31:6
r 2Fa 17:24
s Yos 13:25

tika lango la watu wangu siku
ya maafa yao.[a] Wewe, naam,
wewe, hupaswi kukaza ma-
cho juu ya msiba wake siku
ya maafa yake; wala kunyoo-
sha mkono wako juu ya mali
yake siku ya maafa yake.[b]
14 Nawe hupaswi kusimama
kwenye makutano ya njia, ili
kukatilia mbali watu wake wa-
lioponyoka;[c] wala kuwakabi-
dhi waokokaji wake siku ya ta-
abu.[d] **15** Kwa maana siku ya
Yehova juu ya mataifa yote iko
karibu.[e] Kama ulivyofanya,
ndivyo utakavyofanyiwa.[f] Ma-
tendo yako yatakurudia juu
ya kichwa chako mwenyewe.[g]
16 Kwa maana kama ninyi
mlivyokunywa kwenye mlima
wangu mtakatifu, ndivyo ma-
taifa yote watakavyoendelea
kunywa daima.[h] Nao watuku-
nywa na kumeza wawe kana
kwamba hawakupata kuwapo
kamwe.

17 "Na katika Mlima Sayu-
ni ndipo watakapokuwa wale
wanaoponyoka,[i] nao uta-
kuwa kitu kitakatifu;[j] na nyu-
mba ya Yakobo itamiliki mali
yao.[k] **18** Na nyumba ya Ya-
kobo itakuwa moto,[l] nyumba
ya Yosefu itakuwa mwali wa
moto, nyumba ya Esau itaku-
wa kama majani makavu;[m] nao
watayateketeza na kuyame-
za. Na hakutakuwapo waoko-
kaji katika nyumba ya Esau;[n]
kwa maana Yehova mwenye-
we amesema hayo. **19** Nao
watamiliki Negebu, eneo le-
nye milima la Esau,[o] na Shefe-
la, ya Wafilisti.[p] Nao watamili-
ki shamba la Efraimu[q] na sha-
mba la Samaria;[r] na Benyami-
ni atamiliki Gileadi.[s] **20** Nao

wahamishwa wa boma hili,[a] wana wa Israeli, eneo lililomilikiwa na Wakanaani[b] mpaka Sarefathi[c] litakuwa lao. Na wahamishwa wa Yerusalemu, waliokuwa katika Sefaradi, watamiliki majiji ya Negebu.[d]

a Zb 122:7
b Mwa 13:7
Zek 14:21
c 1Fa 17:9
Lu 4:26
d Yer 13:19
Yer 33:13

21 "Na waokozi[a] watapanda Mlima Sayuni,[b] ili kuhukumu eneo lenye milima la Esau;[c] na lazima ufalme utakuwa wa Yehova."[d]

Safu ya 2 a Ne 9:27; Zb 2:6; Isa 19:20; Ufu 7:4; b Yer 31:6; Yoe 2:32; c Zb 149:7; Eze 35:11; d Zb 22:28; Zek 14:9.

YONA

1 Neno la Yehova likaanza kumjia Yona[a] mwana wa Amitai, na kusema: **2** "Ondoka, uende Ninawi[b] lile jiji kubwa, ukalitangazie kwamba ubaya wao umefika mbele zangu."[c]

3 Naye Yona akasimama na kukimbia kwenda Tarshishi[d] kutoka mbele za Yehova;[e] mwishowe akafika Yopa[f] na kupata meli inayokwenda Tarshishi. Basi akatoa malipo yake ya kusafiri, akashuka chini ndani ya meli, apate kwenda pamoja nao Tarshishi kutoka mbele za Yehova.

4 Na Yehova mwenyewe akavumisha upepo mkubwa baharini,[g] kukawa na tufani kubwa[h] baharini; nayo meli ikawa karibu kuvunjika. **5** Nao wanamaji wakaanza kuogopa na kuomba msaada, kila mmoja kwa mungu wake.[i] Nao wakawa wakitupa baharini vyombo vilivyokuwa ndani ya meli, ili kuipunguzia uzito wake.[j] Lakini Yona alikuwa ameshuka na kuingia sehemu za ndani kabisa za chombo hicho chenye ghorofa, naye akajilaza chini, akalala usingizi mzito.[k] **6** Mwishowe kapteni wa meli akamkaribia na kumwambia: "Una nini wewe, mwenye kulala usingizi? Simama, mwite mungu wako![a] Huenda Mungu wa kweli ataonyesha kuwa anatujali, nasi hatutaangamia."[b]

7 Nao wakaanza kusemezana: "Njooni, tupige kura,[c] tupate kujua ni kwa sababu ya nani tuna taabu hii."[d] Nao wakaendelea kupiga kura, mwishowe kura ikamwangukia Yona.[e] **8** Basi wakamwambia: "Tafadhali tuambie, ni kwa sababu ya nani tuna taabu hii?[f] Unafanya kazi gani, nawe unatoka wapi? Unatoka nchi gani, nawe umetoka kwa watu wa taifa gani?"

9 Ndipo akawaambia: "Mimi ni Mwebrania,[g] nami namwogopa[h] Yehova Mungu wa mbinguni,[i] Yeye aliyeifanya bahari na nchi kavu."[j]

10 Na watu hao wakaanza kuogopa sana, wakamwambia: "Ni nini hili ambalo umefanya?"[k] Kwa maana watu hao walikuwa wamepata kujua kwamba alikuwa akikimbia kutoka mbele za Yehova, kwa sababu alikuwa amewaambia. **11** Mwishowe wakamwambia: "Tukufanyie nini,[l] ili bahari

SURA 1
a 2Fa 14:25
Lu 11:29
b Mwa 10:11
Nah 1:1
Sef 2:13
Mt 12:41
c Mwa 18:20
Yak 5:4
Ufu 18:5
d Mwa 10:4
2Nya 9:21
Isa 23:1
Yer 10:9
e Ebr 10:38
f Yos 19:46
Mdo 9:36
Mdo 10:5
g Zb 78:26
Amo 4:13
h Zb 107:25
Mdo 27:14
i Zb 96:5
Isa 41:29
1Ko 8:4
j Mdo 27:18
Mdo 27:38
k Mt 8:24

Safu ya 2
a Zb 107:6
b Yon 3:9
c Met 16:33
Met 18:18
Mdo 13:19
d Yos 7:14
1Sa 14:42
e Yos 7:18
f Yos 7:19
1Sa 14:43
g Mwa 14:13
Mwa 40:15
h Mhu 12:13
Ufu 15:4
i Zb 103:19
Zb 115:16
Zb 136:26
j Ne 9:6
Zb 95:5
Zb 146:6
Mdo 14:15
k Yos 7:25
Zb 96:4
l 2Sa 21:3

itulie kwa ajili yetu?” Kwa maana bahari ilikuwa ikizidi kuchafuka. **12** Basi akawaambia: “Mninyanyue na kunitupa baharini, nayo bahari itatulia kwa ajili yenu; kwa maana najua kwamba ni kwa sababu yangu tufani hii kubwa imewajia.”[a] **13** Lakini watu hao wakajaribu kupasua njia, wapate kuirudisha meli kwenye nchi kavu; hata hivyo hawakuweza, kwa sababu bahari ilikuwa ikizidi kuwachafukia.[b]

14 Nao wakaanza kumwita Yehova na kusema:[c] “Ah, sasa, Ee Yehova, tafadhali, tusiangamie kwa sababu ya nafsi ya mtu huyu! Nawe usiweke juu yetu damu isiyo na hatia,[d] kwa kuwa wewe mwenyewe, Ee Yehova, umefanya ulivyopenda!”[e] **15** Ndipo wakamnyanyua Yona, wakamtupa baharini; na bahari ikaanza kutulia, ikaacha kuchafuka.[f] **16** Halafu watu hao wakaanza kumwogopa sana Yehova,[g] na hivyo wakamtolea Yehova dhabihu[h] na kuweka nadhiri.[i]

17 Sasa Yehova akamweka samaki mkubwa ammeze Yona,[j] naye Yona akawa katika tumbo la samaki huyo siku tatu mchana na usiku.[k]

2 Ndipo, kutoka ndani ya tumbo la samaki huyo, Yona akasali kwa Yehova Mungu wake[l] **2** na kusema:

“Katika taabu yangu
nilimwita Yehova,[m] naye akanijibu.[n]
Katika tumbo la Kaburi*
nilililia msaada.[o]
Ulisikia sauti yangu.[p]
3 Uliponitupa kwenye
vilindi, ndani ya moyo
wa bahari kuu,[a]
Ndipo mto nao
ukanizunguka.
Mashuu yako yote
na mawimbi yako—
yalipita juu yangu.[b]
4 Nami nikasema,
‘Nimefukuzwa kutoka
mbele za macho yako![c]
Nitapataje kuliona tena
hekalu lako takatifu?’[d]
5 Maji yalinizunguka mpaka
katika nafsi;[e] kilindi cha
maji nacho kikazidi
kunizunguka.
Magugu yalinizunguka
kichwani.
6 Nilishuka mpaka sehemu
za chini kabisa za
milima.
Nayo dunia, mapingo yake
yalikuwa juu yangu
mpaka wakati usio na
kipimo.
Lakini uliinua uhai wangu
toka shimoni, Ee Yehova
Mungu wangu.[f]
7 Nafsi yangu ilipozimia
ndani yangu,[g] Yehova
Ndiye niliyemkumbuka.[h]
Ndipo sala yangu ikaingia
kwako, ndani ya hekalu
lako takatifu.[i]
8 Nao wale wanaozifuata
sanamu zisizo za kweli,
wanaziacha fadhili zao
wenyewe zenye upendo.[j]
9 Lakini mimi, kwa sauti
ya kutoa shukrani
nitakutolea dhabihu.[k]
Nilichoweka nadhiri,
nitakitimiza.[l] Wokovu
ni wa Yehova.”[m]
10 Baadaye Yehova akamwamuru huyo samaki, akamtapika Yona kwenye nchi kavu.[n]

Yon 2:2* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

SURA 1
a 2Sa 24:17; 1Nya 21:17; Zb 25:9
b Zb 107:25
c Zb 65:2; Zb 107:28; Isa 26:16
d Mwa 9:6; Kum 21:8
e Zb 115:3; Zb 135:6; Da 4:35
f Zb 65:7; Zb 89:9; Zb 107:29; Mt 8:26
g Da 6:26; Mdo 5:11
h Zb 50:15
i Mwa 28:20; Zb 50:14
j Mwa 1:21; Zb 104:25
k Mt 12:40; Mt 16:4; Lu 11:30

SURA 2
l 2Nya 33:13; Zb 91:15; Isa 26:16; Ho 5:15
m Zb 130:1; Omb 3:55
n Zb 22:24; Zb 120:1
o Zb 16:10; Mt 12:40; Mdo 2:27
p Zb 18:6; Zb 34:6

Safu ya 2
a Zb 69:1
b Zb 42:7
c Zb 31:22
d 1Fa 8:38; 2Nya 6:38; Zb 5:7
e Zb 69:1
f Ayu 33:24; Zb 16:10; Zb 30:3; Isa 38:17; Mdo 2:31
g Zb 119:81; Zb 142:3
h Zb 77:11; Zb 143:5; 2Ko 1:9
i 2Nya 30:27; Zb 18:6
j 1Sa 12:21; Yer 16:19; Hab 2:18; 1Ko 12:2
k Zb 50:14; Ho 14:2; Ro 12:1; Ebr 13:15
l Mhu 5:4
m Zb 3:8; Isa 12:2
n Zb 33:9; Isa 50:2

3 Ndipo neno la Yehova likamjia Yona mara ya pili, na kusema:[a] **2** "Ondoka, uende Ninawi lile jiji kubwa, ukalitangazie neno[b] ninalokuambia."

3 Basi Yona akasimama na kwenda Ninawi kulingana na neno la Yehova.[c] Sasa Ninawi lilikuwa jiji kubwa kwa Mungu,[d] lenye mwendo wa kutembea wa siku tatu. **4** Mwishowe Yona akaanza kuingia jijini mwendo wa kutembea wa siku moja, naye aliendelea kutangaza na kusema: "Bado siku 40 tu, na Ninawi litaangamizwa."[e]

5 Nao watu wa Ninawi wakaanza kumwamini Mungu,[f] ndipo wakatangaza kufunga na kuvaa nguo za magunia,[g] kutoka aliye mkubwa zaidi kati yao mpaka aliye mdogo zaidi. **6** Neno hilo lilipomfikia mfalme wa Ninawi,[h] ndipo akasimama kutoka kwenye kiti chake cha ufalme, akavua vazi lake rasmi na kujifunika nguo za magunia na kuketi katika majivu.[i] **7** Zaidi ya hayo, akaagiza mwito utolewe, naye akaagiza utolewe katika Ninawi, kwa agizo la kisheria la mfalme na wakubwa wake, na kusema:

"Hakuna mwanadamu wala mnyama wa kufugwa, mifugo wala kundi, anayepaswa kuonja kitu chochote. Yeyote asile chakula. Hata maji wasinywe.[j] **8** Nao wajifunike nguo za magunia, mwanadamu na mnyama wa kufugwa; na wamwite Mungu kwa nguvu na warudi,[k] kila mmoja kutoka katika njia yake mbaya na kutoka katika jeuri iliyokuwa mikononi mwao. **9** Ni nani anayejua iwapo Mungu wa kweli hatageuka na kujuta[a] na kuacha hasira yake inayowaka, tusije tukaangamia?"[b]

10 Naye Mungu wa kweli akaona matendo yao,[c] kwamba walikuwa wamegeuka kutoka katika njia yao mbaya;[d] naye Mungu wa kweli akajuta[e] juu ya msiba ambao alikuwa amesema ataleta juu yao; naye hakuuleta.[f]

4 Hata hivyo, jambo hilo halikumpendeza[g] Yona hata kidogo, naye akawaka hasira. **2** Kwa hiyo akasali kwa Yehova na kusema: "Ah, sasa, Ee Yehova, je, hili halikuwa hangaiko langu, nilipokuwa katika nchi yangu mwenyewe? Ndiyo sababu nilikimbia na kwenda Tarshishi;[h] kwa maana nilijua kwamba wewe ni Mungu mwenye neema na rehema,[i] si mwepesi wa hasira na ni mwingi wa fadhili zenye upendo,[j] na mwenye kuujuta msiba.[k] **3** Na sasa, Ee Yehova, tafadhali, iondoe nafsi yangu[l] kutoka kwangu, kwa maana ni afadhali mimi nife kuliko niwe hai."[m]

4 Naye Yehova akasema: "Je, umewaka hasira kwa haki?"[n]

5 Ndipo Yona akaenda nje ya jiji na kuketi upande wa mashariki wa jiji; mwishowe akajitengenezea kibanda hapo, ili apate kuketi chini yake katika kivuli[o] mpaka aone litakalolipata jiji hilo.[p] **6** Kwa hiyo Yehova Mungu akaweka mtango, kwamba uje juu ya Yona, uwe kivuli juu ya kichwa chake, ili kumwokoa kutoka kati-

SURA 3
a Yon 1:1
b Yon 1:2
c Eze 9:11
Yon 2:9
d Mwa 10:11
Yon 4:11
e Yer 18:7
Sef 2:13
f Kut 9:20
Mt 12:41
Lu 11:32
g 2Nya 20:3
Ezr 8:21
Yoe 1:13
h Zb 2:10
i Da 9:3
Mt 11:21
Mt 12:41
j Ezr 8:21
k Isa 1:16
Eze 18:21
Yoe 2:12
Mt 3:8
Mdo 3:19

Safu ya 2
a Yoe 2:13
b Yer 18:8
c 2Nya 16:9
d Lu 11:32
e Eze 18:23
Yon 4:2
f Yer 18:8

SURA 4
g Mt 20:15
Ro 12:16
Yak 4:5
h Yon 1:3
i Kut 34:6
Zb 103:8
Zb 145:8
Yoe 2:13
j Zb 78:38
Zb 86:5
Mik 7:18
k Yer 18:8
Eze 33:11
Amo 7:3
l Mwa 35:18
m Hes 11:15
1Fa 19:4
Ayu 6:9
n Mt 20:15
o 1Fa 19:4
p Yon 3:4

ka hali yake ya taabu.[a] Na Yona akaanza kushangilia sana juu ya mtango huo.

7 Lakini Mungu wa kweli akaweka mdudu[b] wakati wa mapambazuko ya kesho yake, ili aushambulie mtango huo; mwishowe ukakauka.[c] **8** Na ikawa kwamba, mara jua lilipoangaza, Mungu akaweka pia upepo wenye kukausha wa mashariki[d] na jua likazidi kukichoma kichwa cha Yona, hivi kwamba akawa anazimia;[e] akaendelea kuomba kwamba nafsi yake ife. Akasema kwa kurudia-rudia: "Afadhali mimi nife kuliko niwe hai."[f]

9 Naye Mungu akamwambia Yona: "Je, ni kwa haki wewe kuwaka hasira juu ya mtango huo?"[a]

Ndipo akasema: "Ni kwa haki mimi kuwaka hasira, kiasi cha kufa." **10** Lakini Yehova akasema: "Wewe, kwa upande wako, uliusikitikia mtango, ambao hukuufanyia kazi ya taabu wala kuukuza, ambao ulikuwa mmea tu ulioota usiku mmoja na kuangamia kama mmea tu ulioota usiku mmoja. **11** Na mimi, kwa upande wangu, je, sipaswi kusikitikia Ninawi lile jiji kubwa,[b] ambalo lina wanadamu zaidi ya 120,000 wasiojua hata kidogo tofauti kati ya mkono wao wa kuume na wa kushoto, na tena wanyama wengi wa kufugwa?"[c]

SURA 4
a Zb 103:10; Zb 103:13; Zb 121:5
b Kum 28:39
c Isa 40:7
d Eze 17:10; Eze 19:12; Ho 13:15
e Amo 8:13
f Yon 4:3

Safu ya 2
a Yon 4:4
b Yon 3:3; Mt 18:33
c Zb 36:6; Zb 145:9

MIKA

1 Neno la Yehova lililomjia Mika[a] wa Moreshethi, katika siku za Yothamu,[b] Ahazi,[c] Hezekia,[d] wafalme wa Yuda,[e] ambalo aliona katika maono kuhusu Samaria[f] na Yerusalemu:[g]

2 "Sikieni, enyi vikundi vya watu, ninyi nyote; kazeni uangalifu, Ee dunia na vyote vinavyokujaza,[h] naye Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova na awe shahidi juu yenu,[i] Yehova katika hekalu lake takatifu.[j] **3** Maana, tazama! Yehova anatoka mahali pake,[k] naye atashuka na kukanyaga mahali pa juu pa dunia.[l] **4** Na milima itayeyuka chini yake,[m] na nchi tambarare za chini zitapasuka, kama nta kwa sababu ya moto,[a] kama maji yanayomwagwa kwenye mteremko mkali.

5 "Ni kwa sababu ya maasi ya Yakobo kwamba kuna hayo yote, kwa sababu ya dhambi za nyumba ya Israeli.[b] Maasi ya Yakobo ni nini? Je, si Samaria?[c] Ni mahali gani pa juu pa Yuda?[d] Je, si Yerusalemu? **6** Nami nitalifanya Samaria kuwa rundo la mabomoko ya shambani,[e] mahali pa kupanda mizabibu; nami nitamwaga mawe yake katika bonde, na misingi yake nitaifunua.[f] **7** Na

SURA 1
a Yer 26:18
b 2Fa 15:7; 2Fa 15:32; 1Nya 3:12; 2Nya 27:1
c 2Fa 16:2; 2Nya 28:1; Isa 7:1; Ho 1:1
d 2Fa 18:1; 2Nya 29:1; Isa 36:1
e Isa 1:1
f 1Fa 16:24; Amo 4:1
g Mik 3:10
h Isa 1:2
i Zb 50:7; Mal 3:5
j Zb 11:4; Hab 2:20
k Zb 115:3; Isa 26:21; Eze 3:12
l Kum 32:13; Kum 33:29; Amo 4:13
m Amu 5:5; Zb 97:5

Safu ya 2 a 2Pe 3:10; b 2Fa 17:7; Yer 2:17; c Ho 7:1; d 2Fa 16:4; e 2Fa 19:25; f Eze 13:14; Mt 24:2.

sanamu zake zote za kuchongwa zitavunjwa vipande-vipande,[a] na zawadi zote alizopewa kuwa malipo yake zitateketezwa katika moto;[b] na sanamu zake zote nitazifanya kuwa mahame yaliyo ukiwa. Maana alizikusanya kutoka kwa vitu vilivyotolewa kuwa malipo ya kahaba, nazo zitarudi zikiwa kitu kilichotolewa kuwa malipo ya kahaba."[c]

8 Kwa sababu hiyo nitaomboleza na kupiga mayowe;[d] nitatembea miguu wazi na uchi.[e] Nitaomboleza kama mbwa-mwitu, na kuomboleza kama mbuni-jike. **9** Maana jeraha lililo juu yake haliwezi kupona;[f] maana limefika mpaka Yuda,[g] pigo hilo limefika mpaka lango la watu wangu, mpaka Yerusalemu.[h]

10 "Msiseme hili katika Gathi; msilie hata kidogo.[i]

"Katika nyumba ya Afra gaagaa mavumbini.[j] **11** Vuka, Ee mwanamke mkaaji wa Shafiri, katika uchi wenye aibu.[k] Mwanamke mkaaji wa Saanani hajaondoka. Maombolezo ya Beth-ezeli yatawaondolea ninyi mahali pake pa kusimama. **12** Maana mwanamke mkaaji wa Marothi amengojea mema,[l] lakini mabaya yameshuka kutoka kwa Yehova mpaka kwenye lango la Yerusalemu.[m] **13** Funga gari kwenye kikundi cha farasi, Ee mwanamke mkaaji wa Lakishi.[n] Yeye alikuwa mwanzo wa dhambi kwa binti Sayuni,[o] maana ndani yako maasi ya Israeli yamepatikana.[p] **14** Kwa hiyo utampa Moresheth-gathi zawadi za kuaga.[a] Nyumba za Akzibu[b] zilikuwa kama kitu chenye udanganyifu kwa wafalme wa Israeli. **15** Bado nitakuletea mnyang'anyi,[c] Ee mwanamke mkaaji wa Maresha.[d] Utukufu wa Israeli utakuja mpaka Adulamu.[e] **16** Fanya upara, unyoe nywele zako kwa sababu ya wana wa furaha yako tele.[f] Panua upara wako kama ule wa tai, kwa sababu wameondoka kwako kwenda uhamishoni."[g]

2 "Ole wao wanaopanga mambo yenye kudhuru, na wale wanaozoea kufanya lililo baya, vitandani mwao![h] Wao hulifanya kwenye nuru ya asubuhi,[i] kwa sababu hilo liko katika uwezo wa mikono yao.[j] **2** Nao wametamani mashamba na kuyanyakua;[k] nyumba pia, nao wamezichukua; nao wamempunja mwanamume na nyumba yake,[l] mtu na fungu lake la urithi.[m]

3 "Kwa hiyo Yehova amesema hivi, 'Tazama, nakusudia msiba[n] juu ya familia hii[o] ambao hamtaziondoa shingo zenu[p] ndani yake, ili msitembee kwa majivuno;[q] kwa sababu ni wakati wa msiba.[r] **4** Siku hiyo mtu atapaaza neno la kimethali[s] kuwahusu ninyi naye ataomboleza, ndiyo, maombolezo.[t] Mtu atasema: "Hakika tumeporwa![u] Anabadili fungu la watu wangu.[v] Jinsi anavyoliondoa kwangu! Anawagawia wasio waaminifu mashamba yetu wenyewe." **5** Kwa hiyo hutakuwa na yeyote anayetu-

SURA 1
a Law 26:30 Ho 8:6
b Ho 2:5 Ho 9:1
c Kum 23:18
d Yer 4:19
e Isa 20:2
f Isa 1:5 Yer 15:18
g 2Fa 18:13 Isa 8:8
h 2Nya 32:2 Mik 1:12
i 2Sa 1:20
j Yer 6:26 Eze 27:30
k Isa 47:3 Yer 13:26 Eze 16:37
l Isa 59:9 Yer 8:15
m Isa 45:7 Amo 3:6
n Yos 15:39 2Fa 18:14
o 1Fa 14:16
p 2Fa 16:3 Yer 3:8

Safu ya 2
a 2Fa 15:19
b Yos 15:44
c Isa 7:17
d 2Nya 11:8
e Mwa 38:1 Ne 11:30
f Ayu 1:20 Isa 15:2 Isa 22:12 Yer 7:29
g Kum 28:41 2Fa 17:6 Isa 39:7

SURA 2
h Est 3:8 Zb 36:4 Lu 22:2
i Ho 7:6 Mt 27:1 Mdo 23:12
j Mwa 31:29 1Fa 21:7 Yoh 19:10
k Kut 20:17 1Fa 21:2 Ne 5:11 Isa 5:8 Eze 22:29
l Yer 22:17 Eze 18:12 Eze 22:12
m Ne 5:5
n Yer 18:11 Yak 2:13
o Yer 8:3 Amo 3:1
p Amo 2:14
q Isa 2:11 Da 5:20 1Pe 5:5
r Amo 5:13
s Hes 23:18 Ayu 27:1 Hab 2:6
t Yer 9:10 Omb 1:1 Eze 2:10

u Isa 6:11; Yer 25:9; Sef 1:2; v 2Fa 17:23.

pa kamba, kwa kura,[a] katika
kutaniko la Yehova. **6** Ninyi
msiache maneno yaanguke.[b]
Wanaacha maneno yaanguke.
Hawataacha maneno yaanguke
kuhusu mambo haya. Fedheha
hazitaondoka.[c]

7 "'Je, inasemwa, Ee nyu-
mba ya Yakobo:[d] "Roho ya Ye-
hova imekosa kuridhika, au
haya ndiyo matendo yake?"[e]
Je, maneno yangu mwenye-
we hayafanyi mema[f] kwa yeye
anayetembea kwa unyoofu?[g]

8 "'Na jana watu wangu
mwenyewe walisimama kama
adui mkaidi.[h] Vueni pambo le-
nye utukufu kutoka mbele
ya vazi, kutoka kwa wale wa-
naopita wakiwa na uhakika,
kama wale wanaorudi kutoka
vitani. **9** Mnawafukuza wa-
nawake wa watu wangu ku-
toka katika nyumba amba-
mo mwanamke ana furaha
tele. Mnachukua utukufu wa-
ngu[i] kutoka kwa watoto wake,
mpaka wakati usio na kipimo.[j]
10 Ondoka uende,[k] kwa saba-
bu hapa si mahali pa kupu-
mzika.[l] Kwa sababu ya uhaki-
ka wa kwamba amekuwa asi-
ye safi,[m] kuna kuvunja-vunja;
na kazi hiyo ya kuvunja-vu-
nja ina maumivu.[n] **11** Ikiwa
mwanamume, anayetembea
akifuata upepo na uwongo,
amesema uwongo:[o] "Nitakua-
ngushia maneno kuhusu divai
na kuhusu kileo," yeye pia ata-
kuwa yule anayewaangushia
watu hawa maneno.[p]

12 "'Hakika nitamkusanya
Yakobo, ninyi nyote;[q] bila sha-
ka nitawakusanya pamoja wa-
naobaki wa Israeli.[r] Nitawaa-
nganisha, kama kundi zizini,
kama kundi la wanyama ka-
tikati ya malisho yake;[a] huko
kutakuwa na kelele za wana-
damu.'[b]

13 "Anayepenyeza atakuja
mbele yao:[c] watapenya. Nao
watapita kati ya lango, nao
watatoka nje kwa hilo.[d] Na
mfalme wao atapita kati mbe-
le yao, Yehova akiwa mbele
yao."[e]

3 Nami nikasema: "Tafadha-
li sikieni, ninyi vichwa vya
Yakobo na ninyi viongozi wa
nyumba ya Israeli.[f] Je, si waji-
bu wenu kujua haki?[g] **2** Ni-
nyi mnaochukia yaliyo mema[h]
na mnaopenda ubaya,[i] mnao-
chuna ngozi kutoka kwa watu
na nyama kutoka kwa mi-
fupa yao;[j] **3** ninyi ambao pia
mmekula nyama ya watu wa-
ngu,[k] na mmeichuna ngozi yao
kutoka kwao, mkaivunja vi-
pande-vipande mifupa yao,
na kuiponda vipande-vipande
kama kitu kilicho katika chu-
ngu chenye mdomo mpana na
kama nyama ndani ya chungu
cha kupikia.[l] **4** Wakati huo
watamwomba Yehova msaada,
lakini hatawajibu.[m] Naye ata-
ficha uso wake kutoka kwao
wakati huo,[n] kulingana na wa-
livyotenda ubaya kwa mate-
ndo yao.[o]

5 "Yehova amesema hivi juu
ya manabii ambao wanawapote-
za watu wangu,[p] ambao wana-
uma kwa meno yao[q] na ambao
hupaaza sauti, 'Amani!'[r] ambao,
mtu yeyote asipoweka kitu vi-
nywani mwao, pia hutakasa
vita juu yake,[s] **6** 'Basi ninyi
mtakuwa na usiku,[t] kusiweko

SURA 2

a Hes 26:55
Zb 78:55
b Eze 21:2
Mdo 4:17
c Yer 6:15
Yer 8:12
d Yer 2:4
e Kum 32:4
Isa 50:2
f Zb 19:7
Zb 33:4
Yer 15:16
g Zb 15:2
Met 2:7
h Isa 9:21
i Eze 16:14
j Yoe 3:6
k Yos 23:15
l Kum 12:9
m Law 18:25
Zb 106:38
n Yer 9:19
Yer 10:18
o 1Fa 22:6
Isa 9:15
Yer 6:14
Eze 13:3
1Yo 4:1
p 2Th 2:11
q Isa 11:11
Yer 31:8
Mik 4:6
r Yer 23:3

Safu ya 2

a Eze 34:11
b Eze 36:38
Zek 8:22
c Isa 45:1
Isa 59:16
d Isa 62:10
e Isa 42:13
Isa 49:10
Isa 52:12
Zek 9:14
Zek 10:5

SURA 3

f Mik 3:9
g Kum 1:13
1Ko 6:5
h 1Fa 22:8
Amo 5:10
Lu 19:14
i 2Nya 19:2
Met 28:4
j Eze 22:27
Amo 8:4
Sef 3:3
k Zb 53:4
Eze 34:3
l Isa 5:15
m Met 1:28
Isa 1:15
Yoh 9:31
n Kum 31:17
Yer 33:5
Omb 3:44
o Isa 3:11
Ro 2:8
p Isa 9:16
Isa 56:10
Eze 13:10
Mt 15:14
q Eze 13:19
Eze 34:2
Mt 7:15
Ro 16:18
r Yer 23:17
Eze 13:10
s Zb 55:3
Zb 120:7
Zb 140:2

t Isa 8:20; Yer 13:16.

maono;[a] nanyi mtakuwa na giza, ili msifanye uaguzi. Nalo jua litatua juu ya manabii, na mchana utakuwa mweusi juu yao.[b] **7** Waonaji[c] watakata tamaa. Nao wote watafunika masharubu,[f] kwa maana hakuna jibu kutoka kwa Mungu.'"[g]

8 Nami nimejaa nguvu, kwa roho ya Yehova, na ya haki na uwezo,[h] ili nimwambie Yakobo maasi yake na Israeli dhambi yake.[i]

9 Tafadhali sikieni hili, ninyi vichwa vya nyumba ya Yakobo nanyi viongozi wa nyumba ya Israeli,[j] mnaochukia haki na mnaopotoa hata kila kitu ambacho kimenyooka;[k] **10** mnaojenga Sayuni kwa matendo ya umwagaji wa damu na Yerusalemu kwa ukosefu wa uadilifu.[l] **11** Walio vichwa vyake hutoa hukumu ili wale rushwa[m] tu, na makuhani wake hufundisha ili tu wapate malipo,[n] na manabii wake hufanya uaguzi ili tu wapate pesa;[o] hata hivyo wao huendelea kujiegemeza kwa Yehova, wakisema: "Je, Yehova hayuko katikati yetu?[p] Hakuna msiba utakaotupata."[q] **12** Basi kwa sababu yenu Sayuni utalimwa kama shamba, na Yerusalemu litakuwa marundo ya mabomoko,[r] na mlima wa nyumba hiyo utakuwa kama mahali pa juu pa msitu.

4 Na itatukia katika siku za mwisho[s] kwamba mlima[t] wa nyumba[u] ya Yehova utawekwa imara juu ya kilele cha milima, nao utainuliwa juu ya vilima;[v] na vikundi vya watu vitamiminika huko.[a] **2** Na mataifa mengi hakika yatakwenda na kusema: "Njooni,[b] twendeni juu kwenye mlima wa Yehova na kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo;[c] naye atatufundisha njia zake,[d] nasi tutatembea katika mapito yake."[e] Kwa maana sheria itatoka katika Sayuni, na neno la Yehova katika Yerusalemu.[f] **3** Naye hakika atafanya hukumu kati ya vikundi vingi vya watu,[g] na kunyoosha mambo[h] kuhusu mataifa yenye nguvu yaliyo mbali.[i] Nao watafua panga zao ziwe majembe na mikuki yao iwe miundu.[j] Hawatainua upanga, taifa juu ya taifa, wala hawatajifunza vita tena.[k] **4** Nao wataketi, kila mtu chini ya mzabibu wake na chini ya mtini wake,[l] wala hakutakuwa na mtu yeyote anayewatetemesha;[m] kwa maana kinywa cha Yehova wa majeshi kimesema hivyo.[n]

5 Kwa maana vikundi vyote vya watu vitatembea kila kimoja katika jina la mungu wake;[o] bali sisi tutatembea katika jina la Yehova Mungu wetu[p] mpaka wakati usio na kipimo, naam, milele.[q]

6 "Katika siku hiyo," asema Yehova, "nitamkusanya yeye aliyekuwa akichechemea;[r] naye aliyekuwa ametawanywa nitamkusanya pamoja,[s] yeye ambaye nimemtendea vibaya. **7** Nami nitamfanya yeye aliyekuwa akichechemea awe ma-

SURA 3

a Zb 74:9; Eze 13:23
b Isa 59:10; Amo 8:9
c 1Sa 9:9; Isa 29:10
d Zek 13:4
e Isa 44:25
f Eze 24:17
g 1Sa 28:6
h Isa 11:2; Zek 4:6; Mdo 4:8; 1Ko 2:4
i Isa 58:1; Mt 3:7; Mdo 7:51
j Mik 3:1
k Law 26:15; Kum 27:19; Yer 5:28
l Yer 22:13; Hab 2:9; Hab 2:12
m 1Sa 8:3; Isa 1:23; Isa 5:23; Eze 22:12
n Yer 6:13; Tit 1:11
o Isa 56:11; Yud 11
p Isa 48:2; Yer 7:4; Ro 2:17
q Amo 9:10
r Zb 79:1; Yer 26:18; Mik 1:6; Mt 24:2

SURA 4

s Isa 2:2; Da 12:9; Mdo 2:17
t Isa 11:9; Zek 8:3; Ufu 21:10
u 1Pe 2:5
v Isa 2:2

Safu ya 2

a Zb 86:9; Isa 60:3; Ufu 15:4
b Ufu 22:17
c Isa 2:3; Yer 31:6; Zek 8:20
d Kum 6:1; Zb 25:9; Yoh 6:45
e Met 3:6; Isa 2:3; Ebr 12:13
f Zb 128:5
g 1Sa 2:10; Zb 96:13; Isa 51:4; Isa 51:5
h 2Ti 3:16
i Isa 60:12
j Ho 2:18; Zek 9:10
k Zb 72:7; Isa 2:4; Isa 9:7; Isa 60:18; Mt 26:52; Efe 6:12
l 1Fa 4:25; Zek 3:10

m Isa 54:14; Eze 34:25; Eze 39:26; n Isa 55:11; o 2Fa 17:29; Yer 2:11; p Zek 10:12; q Kut 3:15; Zb 48:14; Zb 145:1; r Eze 34:16; Sef 3:19; Ebr 12:12; s Zb 147:2; Isa 56:8; Eze 34:12; Eze 37:21.

baki,[a] na yeye aliyekuwa ameondolewa mbali awe taifa lenye uwezo;[b] na Yehova atatawala juu yao akiwa mfalme katika Mlima Sayuni, kutoka sasa na kuendelea mpaka wakati usio na kipimo.[c]

8 "Wewe nawe, Ee mnara wa kundi, kilima cha binti Sayuni,[d] mpaka kwako itakuja, ndiyo, mamlaka ya kwanza itakuja hakika,[e] ufalme wa binti Yerusalemu.[f]

9 "Basi ni kwa nini unaendelea kupiga kelele?[g] Je, hamna mfalme ndani yako, au je, mshauri wako mwenyewe ameangamizwa, hata maumivu kama yale ya mwanamke anayezaa yakakushika?[h] **10** Ee binti Sayuni, uwe na maumivu makali na utaabike, kama mwanamke anayezaa,[i] maana sasa utaenda kutoka katika mji, nawe utakaa katika shamba.[j] Nawe utaenda mpaka Babiloni.[k] Huko utakombolewa.[l] Huko Yehova atakununua kutoka mkononi mwa adui zako.[m]

11 "Na sasa mataifa mengi yatakusanywa juu yako, wale wanaosema, 'Acheni atiwe uchafu, nayo macho yetu yautazame Sayuni.'[n] **12** Lakini wao nao, hawajapata kujua fikira za Yehova, wala hawajapata kuelewa shauri lake;[o] maana atawakusanya pamoja kwenye uwanja wa kupuria kama mafungu ya nafaka iliyokatwa hivi karibuni.[p]

13 "Simama upure, Ee binti Sayuni;[q] maana nitaibadili pembe yako iwe chuma, na kwato zako nitazibadili ziwe shaba, nawe utaponda kabisa vikundi vingi vya watu;[a] na kwa kupiga marufuku utamtolea Yehova faida yao isiyo ya haki,[b] na mali zao kwa Bwana wa kweli wa dunia yote."[c]

5 "Wakati huu unajikatakata,[d] Ee binti uliyevamiwa; yeye ametuzingira sisi.[e] Watalipiga kwa fimbo shavu la mwamuzi wa Israeli.[f]

2 "Nawe, Ee Bethlehemu Efratha,[g] wewe uliye mdogo sana kuwa kati ya maelfu ya Yuda,[h] kutoka kwako[i] atanijia yeye atakayekuwa mtawala katika Israeli,[j] ambaye asili yake ni kutoka nyakati za kale, kutoka siku za wakati usio na kipimo.[k]

3 "Kwa hiyo atawatoa[l] mpaka wakati ambapo yeye anayezaa anapozaa.[m] Na wale ndugu zake wengine watarudi kwa wana wa Israeli.

4 "Naye atasimama na kuchunga kwa nguvu za Yehova,[n] katika ukuu wa jina la Yehova Mungu wake.[o] Nao wataendelea kukaa,[p] maana sasa atakuwa mkuu mpaka miisho ya dunia.[q] **5** Na huyu atakuwa amani.[r] Lakini wakati Mwashuru atakapokuja katika nchi yetu na kukanyaga juu ya minara yetu ya makao,[s] sisi pia tutasimamisha juu yake wachungaji saba, ndiyo, watawala wadogo wanane kutoka kati ya wanadamu. **6** Nao wataichunga nchi ya Ashuru kwa upanga,[t] na nchi ya Nimrodi[u] katika malango yake. Naye atatukomboa kutoka kwa Mwashuru,[v]

SURA 4
a Isa 10:21; Mik 2:12; Mik 7:18; Ro 9:27; Ro 11:5
b Isa 60:22
c Zb 50:2; Yer 10:10
d 2Sa 5:7; Isa 10:32
e Oba 21
f Zek 9:9; Yoh 12:15
g Yer 8:19
h Zb 48:6; Isa 21:3; Yer 30:6
i Ho 13:13
j Ho 2:14
k 2Fa 20:18; 2Nya 36:20
l Isa 45:13; Zek 2:7
m Zb 106:10; Zb 107:2; Isa 48:20; Yer 15:21
n Omb 2:16; Oba 12; Mik 7:10
o Isa 55:8; Yer 29:11; Ro 11:33
p Isa 21:10; Lu 3:17
q Isa 41:15; Yer 51:33

Safu ya 2
a Zek 9:13
b Yos 6:19; 2Sa 8:11; Isa 18:7; Isa 23:18
c Zek 4:14; Zek 6:5

SURA 5
d Yer 41:5; Yer 48:37
e Kum 28:52; 2Fa 25:1; Lu 19:43
f Mt 26:31; Mt 26:67; Mt 27:30; Mk 14:27; Yoh 18:22; Yoh 19:3
g Mwa 35:19; Lu 2:4
h 1Sa 23:23
i Lu 2:11; Yoh 7:42
j Mwa 49:10; 1Nya 5:2; Isa 9:6; Mt 2:6; Lu 1:32
k Met 8:22; Yoh 1:1; Yoh 8:58; Kol 1:17; Ufu 3:14
l 1Fa 14:16
m Isa 66:8
n Isa 49:9; Eze 34:23; Mik 7:14; Yoh 10:11

o Zb 93:1; Eze 37:24; p Isa 32:18; Yer 23:6; q Zb 72:8; Zek 9:10; Lu 1:33; Ufu 11:15; r Zb 72:7; Isa 9:6; Lu 2:14; s Isa 8:7; t Isa 14:2; Isa 33:1; u Mwa 10:9; Mwa 10:11; v Isa 14:25; Lu 1:71.

anapokuja katika nchi yetu
na anapokanyaga juu ya eneo
letu.
7 "Na mabaki ya Yakobo[a] wa-
takuwa katikati ya makabila
mengi ya watu kama umande
kutoka kwa Yehova,[b] kama ma-
nyunyu mengi ya mvua juu ya
mimea,[c] ambayo hayamtumai-
ni mwanadamu wala kuwango-
jea wana wa mtu wa udongo.[d]
8 Na mabaki ya Yakobo wata-
kuwa kati ya mataifa, katika-
ti ya makabila mengi ya watu,
kama simba katikati ya wa-
nyama wa msituni, kama mwa-
na-simba mwenye manyoya
shingoni katikati ya makundi
ya kondoo, ambaye, anapopita
kati, hukanyaga-kanyaga
na pia hurarua vipande-vipa-
nde;[e] wala hakuna mkombo-
zi. **9** Mkono wako utainuli-
wa juu ya wapinzani wako,[f] na
adui zako wote watakatiliwa
mbali."[g]
10 "Na itatukia katika siku
hiyo," asema Yehova, "kwamba
nitakatilia mbali farasi zako
kutoka katikati yako na kuha-
ribu magari yako.[h] **11** Nami
nitakatilia mbali majiji ya
nchi yako na kubomoa ma-
hali pako pote penye ngome.[i]
12 Nami nitakatilia mbali ulo-
zi kutoka mkononi mwako,
nawe hutaendelea tena kuwa
na watu wowote wanaofanya
uchawi.[j] **13** Nami nitakati-
lia mbali sanamu zako za ku-
chongwa na nguzo zako kuto-
ka katikati yako, nawe hu-
tainamia tena kazi ya miko-
no yako.[k] **14** Nami nitang'oa
miti yako mitakatifu[l] kuto-
ka katikati yako na kuangami-
za majiji yako. **15** Na katika
hasira na ghadhabu nitalipiza
kisasi juu ya mataifa ambayo
hayakutii."[a]
6 Tafadhali, sikieni jambo
ambalo Yehova anasema.[b]
Simameni, endesheni kesi na
milima, vilima na visikie sau-
ti yenu.[c] **2** Sikieni, enyi mili-
ma, sikieni kesi ya Yehova, pia
ninyi vyombo vya kudumu, ni-
nyi misingi ya dunia;[d] kwa ma-
ana Yehova ana kesi na watu
wake, naye atahojiana na Isra-
eli:[e]
3 "Enyi watu wangu,[f] nime-
wafanya nini? Nami nimewa-
chosha kwa njia gani?[g] Toeni
ushuhuda juu yangu.[h] **4** Kwa
maana niliwaleta ninyi kutoka
nchi ya Misri,[i] nami niliwako-
mboa kutoka nyumba ya watu-
mwa;[j] nami nikawatuma Musa,
Haruni na Miriamu[k] mbele
yenu. **5** Tafadhali, enyi watu
wangu, kumbukeni[l] lile amba-
lo Balaki mfalme wa Moabu
alishauri,[m] na lile ambalo Ba-
laamu mwana wa Beori ali-
mjibu.[n] Ilikuwa kutoka Shiti-
mu[o] mpaka Gilgali,[p] kusudi
matendo ya uadilifu ya Yehova
yajulikane."[q]
6 Nitamkaribia Yehova na
nini?[r] Nitajiinamisha na nini
kwa Mungu aliye juu?[s] Je,
nimkaribie na matoleo mazima
ya kuteketezwa,[t] na ndama we-
nye umri wa mwaka mmoja?
7 Je, Yehova atapendezwa na
maelfu ya kondoo-dume, na ma-
kumi ya maelfu ya mito ya ma-
futa?[u] Je, nimtoe mwanangu
mzaliwa wa kwanza kwa aji-

SURA 5
a Eze 14:22
Yoe 2:32
Mik 4:7
Ro 11:5
b Kum 32:2
Zb 110:3
c Zb 72:6
Isa 44:3
1Ko 3:6
d Yer 14:22
e Isa 41:15
Zek 10:5
f Zb 21:8
Isa 26:11
g Lu 19:27
h Zb 20:7
Zb 33:16
Ho 1:7
Ho 14:3
Zek 9:10
i Isa 2:15
j Kum 18:10
Isa 2:6
Isa 8:19
Ufu 22:15
k Isa 2:8
Isa 17:8
Eze 36:25
Ho 14:3
Zek 13:2
l Isa 27:9

Safu ya 2
a Zb 149:7
2Th 1:8

SURA 6
b Yer 13:15
Ebr 1:1
c Zb 50:4
Isa 5:3
Eze 36:1
d Kum 32:22
Zb 50:1
Met 8:29
Isa 1:2
Yer 31:37
e Isa 43:26
Yer 2:35
Ho 4:1
f Zb 81:8
g Yer 2:5
h Isa 43:9
Ro 3:4
i Kut 12:51
Kum 4:20
Mdo 7:36
j Kum 7:8
2Sa 7:23
k Kut 15:20
Hes 12:1
l Kum 9:7
Efe 2:11
m Hes 22:5
Yos 24:9
n Hes 23:7
Hes 24:10
Yos 24:10
2Pe 2:15
Ufu 2:14
o Hes 25:1
Hes 33:49
p Yos 4:19

q Amu 5:11; Zb 71:15; Ro 3:25; r Zb 50:12; Mdo 17:25; s Zb 95:6; Efe 3:14; t 1Sa 15:22; Zb 50:8; Zb 51:16; Isa 1:11; Isa 40:16; Ho 6:6; u Zb 50:10; Zb 51:16; Eze 16:18.

li ya maasi yangu, uzao wa tumbo langu kwa ajili ya dhambi
ya nafsi yangu?[a] **8** Ee mtu wa
udongo, yeye amekuambia ya-
liyo mema.[b] Na Yehova anata-
ka nini kutoka kwako ila ku-
tenda haki[c] na kupenda fadhili[d]
na kuwa na kiasi[e] katika kute-
mbea na Mungu wako?[f]

9 Sauti ya Yehova inaliita
jiji,[g] naye mtu mwenye heki-
ma inayotumika ataliogopa jina
lako.[h] Ninyi isikieni fimbo na
yeye aliyeiweka.[i] **10** Je, bado
kuna hazina za uovu katika
nyumba ya mwovu,[j] na kipi-
mo cha efa kilichobanwa amba-
cho kimeshutumiwa? **11** Je,
naweza kuwa safi kiadili niki-
wa na mizani ya uovu pamo-
ja na mfuko wa mawe ya mizani
ya udanganyifu?[k] **12** Kwa
maana watu wake mwenyewe
walio matajiri wamejaa jeuri,
na wakaaji wake mwenyewe
wamesema uwongo,[l] na ulimi
wao una udanganyifu kinywani
mwao.[m]

13 "Nami pia, nitakufanya
mgonjwa kwa kukupiga;[n] uta-
fanywa ukiwa, kwa sababu
ya dhambi zako.[o] **14** Nawe
utakula wala hutashiba, nawe
utakuwa na njaa.[p] Nawe uta-
ondoa vitu, lakini hutavichu-
kua na kuvipeleka salama; na
chochote ambacho utachukua
na kukipeleka salama, nita-
kitoa kwa upanga.[q] **15** Nawe
utapanda mbegu, bali hutavu-
na. Nawe utakanyaga zeitu-
ni, bali hutajipaka mafuta;
pia divai tamu, bali hutaku-
nywa divai.[r] **16** Na sheria za
Omri[s] na kazi yote ya nyu-
mba ya Ahabu zinafuatwa,[t] na-

SURA 6
a 2Fa 3:27; Zb 49:7; Eze 16:20
b Zb 119:72
c Kum 10:12; Met 21:3; Isa 1:17; Yer 22:3; Eze 45:9; Ho 12:6
d Met 3:3; Met 19:22; Ho 6:6; Zek 7:9; Efe 4:32; Kol 3:12
e Met 8:13; Lu 18:13; Yak 4:6
f Mwa 6:9; Ga 5:22
g Sef 3:2
h Ne 1:11; Met 9:10; Lu 1:17
i Isa 9:13
j Yos 7:1; 2Fa 5:23; Met 10:2; Amo 3:10; Yak 5:3
k Kum 25:13; Met 11:1; Met 20:10; Ho 12:7
l Isa 59:3; Mik 7:2
m Yer 9:3
n Law 26:16; Kum 28:21; Isa 1:5; Mdo 12:23
o Yer 18:16
p Law 26:26; Eze 4:16; Ho 4:10
q Isa 24:17; Eze 5:12
r Kum 28:38; Yer 12:13; Yoe 1:10; Amo 5:11; Hag 1:6
s 1Fa 16:25
t 1Fa 16:30; 2Fa 16:3; 2Fa 21:3

Safu ya 2
a Isa 30:1; Yer 7:24
b Yer 18:16; Yer 19:8
c Zb 44:13; Yer 51:51; Omb 5:1; Da 9:16

SURA 7
d Yer 4:31; Yer 45:3
e Isa 17:6; Isa 24:13; Yer 6:9
f Isa 28:4; Ho 9:10
g Zb 12:1; Zb 14:1; Isa 57:1; Ro 3:10

nyi mnatembea katika masha-
uri yao;[a] ili mimi niwafanye
ninyi kuwa kitu cha kusha-
ngaza na wakaaji wake kuwa
kitu cha kupigiwa mluzi
kwa mshangao;[b] nanyi mta-
chukua shutuma ya vikundi
vya watu."[c]

7 Ole wangu,[d] kwa maana
nimekuwa kama mkusa-
nyo wa matunda ya wakati
wa kiangazi, kama masalio ya
mkusanyo wa zabibu![e] Haku-
na kishada cha zabibu za kula,
hakuna tini ya mapema, amba-
yo nafsi yangu inaweza ku-
tamani![f] **2** Mshikamanifu
ameangamia kutoka dunia-
ni, na kati ya wanadamu ha-
kuna mnyoofu.[g] Wote huvizia
ili kumwaga damu.[h] Huwinda,
kila mmoja ndugu yake mwe-
nyewe, kwa wavu wa kuko-
kota.[i] **3** Mikono yao iko juu
ya lililo baya, ili kulifanya
vema;[j] mkuu anaomba kitu,
naye mwenye kuhukumu hu-
fanya hivyo ili kupata thawa-
bu,[k] na mkubwa anasema ta-
maa iliyo katika nafsi yake
mwenyewe;[l] nao huisokota.
4 Mtu aliye bora zaidi kwao
ni kama mchongoma, aliye
mnyoofu zaidi kwao ni mbaya
kuliko ukuta wa miiba.[m] Siku
ya walinzi wako, siku yenu ya
kukaziwa fikira, itakuja.[n] Sasa
kuhangaishwa kwao kuta-
tokea.[o]

5 Msimwamini mwenzi.
Msimtegemee rafiki msiri.[p] Li-
nda milango ya kinywa chako

h Met 1:11; Met 1:16; Isa 59:7; Ro 3:15; i 1Sa 24:11; Zb 57:6; Hab 1:15; j Met 4:16; Yer 3:5; Yer 4:22; Eze 22:6; k Isa 1:23; Ho 4:18; Mik 3:11; l 1Fa 21:5; m 2Sa 23:6; Eze 2:6; n Isa 10:3; Eze 12:23; Ho 9:7; o Isa 22:5; Lu 21:25; p Ayu 6:15; Zb 118:8; Yer 9:4; Lu 21:16.

kutokana na yeye anayelala
kifuani pako.[a] **6** Kwa maana
mwana anamdharau baba,
binti anasimama kumpinga
mama yake;[b] binti-mkwe ku-
mpinga mama-mkwe wake;[c]
adui za mtu ni watu wa nyu-
mba yake.[d]
7 Lakini mimi, nitaendelea
kumtazamia Yehova.[e] Nitao-
nyesha mtazamo wa kumngo-
jea Mungu wa wokovu wangu.[f]
Mungu wangu atanisikia.[g]
8 Usishangilie juu yangu,
Ee mwanamke adui yangu.[h]
Ijapokuwa nimeanguka, ni-
tasimama;[i] ijapokuwa nina-
kaa gizani,[j] Yehova atakuwa
nuru kwangu.[k] **9** Ghadhabu
ya Yehova nitaivumilia—kwa
maana nimemtendea dha-
mbi[l]—mpaka atakapoende-
sha kesi yangu na kutekeleza
haki kwa ajili yangu.[m] Atani-
leta kwenye nuru; nitautaza-
ma uadilifu wake.[n] **10** Na
adui yangu ataona, aibu ita-
mfunika,[o] yeye aliyekuwa aki-
niambia: "Yuko wapi, Yehova
Mungu wako?"[p] Macho yangu
mwenyewe yatamtazama huyo
mwanamke.[q] Sasa atakuwa
mahali pa kukanyaga-kanya-
ga, kama matope ya barabarani.[r]
11 Siku ya kujenga kuta
zako za mawe, siku hiyo
amri itakuwa mbali kabisa.[s]
12 Siku hiyo watakujia hata
kutoka Ashuru na majiji ya Mi-
sri, na kutoka Misri hata kufi-
ka ule Mto;[t] na kutoka bahari
mpaka bahari, na kutoka mli-
ma mpaka ule mlima.[u] **13** Na
nchi itakuwa mahame yenye
ukiwa kwa sababu ya wakaaji
wake, kwa sababu ya matunda
ya matendo yao.[a]
14 Wachunge watu wako
kwa fimbo yako,[b] kundi la uri-
thi wako, yeye aliyekuwa aki-
kaa peke yake msituni—kati-
kati ya shamba la matunda.[c]
Na walishe katika Bashani na
Gileadi[d] kama katika siku za
zamani.[e]
15 "Nitamwonyesha ma-
mbo ya ajabu kama katika zile
siku ulipokuwa ukitoka nchi
ya Misri.[f] **16** Mataifa yatao-
na na kuonea aibu uwezo
wao wote.[g] Wataweka mko-
no wao juu ya vinywa vyao;[h]
masikio yao yatakuwa na uzi-
wi. **17** Wataramba mavumbi
kama nyoka;[i] kama watamba-
aji wa dunia watatoka katika
maboma[j] yao wakitetemeka.
Watamjia Yehova Mungu wetu
wakitetemeka, nao watakuo-
gopa."[k]
18 Ni nani aliye Mungu
kama wewe,[l] anayesamehe
kosa na kuuachilia ukosaji[m]
wa mabaki ya urithi wake?[n]
Hatashikilia hasira yake mi-
lele, kwa maana yeye hupe-
ndezwa na fadhili zenye upe-
ndo.[o] **19** Atatuonyesha rehe-
ma tena;[p] atayatiisha makosa
yetu.[q] Nawe utazitupa dha-
mbi zao zote[r] katika vilindi
vya bahari. **20** Utatoa ukwe-
li aliopewa Yakobo, fadhili ze-
nye upendo alizopewa Abraha-
mu, ambazo uliwaapia mababu
zetu tangu siku za zamani za
kale.[s]

SURA 7

a Amu 16:18
b Met 30:11
Eze 22:7
Mt 10:21
Lu 21:16
c Lu 12:53
2Ti 3:2
d Zb 41:9
Yer 12:6
Mt 10:36
Yoh 13:18
e Zb 34:5
Zb 123:2
Isa 8:17
f Mwa 49:18
Zb 25:5
Zb 62:1
Omb 3:26
Lu 2:25
g Zb 4:3
Zb 40:1
Zb 65:2
Isa 12:2
Isa 25:9
1Yo 5:14
h Eze 25:6
Ufu 11:10
i Zb 37:24
Met 24:16
j Zb 107:10
k Zb 27:1
Lu 1:78
2Ko 4:6
l Omb 1:18
Lu 15:18
m 1Sa 24:15
Ufu 18:20
n Zb 37:6
1Ko 4:5
2Th 1:10
o Zb 35:26
p Zb 42:3
Zb 79:10
Zb 115:2
Da 3:15
Yoe 2:17
Mt 27:43
q Zb 58:10
r 2Sa 22:43
s Ne 2:17
t Mwa 15:18
u Isa 11:16
Isa 27:13
Ho 11:11

Safu ya 2

a Law 26:33
Yer 21:14
Yer 25:11
Lu 21:24
Ga 6:7
b Zb 23:1
Zb 28:9
Isa 40:11
Yoh 10:27
c Isa 37:24
d Yer 50:19
Eze 34:23
e Mal 3:4
f Zb 78:12
Isa 63:11
Yer 23:7

g Zb 126:2; Isa 26:11; Isa 66:18; **h** Ayu 29:9; Isa 52:15; **i** Zb 72:9; Isa 49:23; **j** Zb 18:45; **k** Yos 2:9; Yer 33:9; **l** Kut 15:11; Zb 35:10; Isa 40:18; **m** Kut 34:7; Ne 9:17; Zb 65:3; Zb 86:5; Isa 1:18; Isa 44:22; Yer 50:20; Da 9:9; **n** Yer 23:3; Yoe 2:32; Ro 9:27; Ufu 12:17; **o** Zb 36:7; Zb 62:12; Zb 103:9; Isa 57:16; Omb 3:22; **p** Kum 30:3; Zb 103:13; Da 9:9; Ho 2:19; Efe 2:4; **q** Zb 130:8; **r** Zb 103:12; Isa 38:17; Isa 55:7; Yer 31:34; Yer 50:20; **s** Mwa 22:17; Zb 105:9; Lu 1:72; Mdo 3:25; Ebr 6:13.

NAHUMU

1 Tangazo juu ya Ninawi:[a] Kitabu cha maono ya Nahumu Mwelkoshi:

2 Yehova ni Mungu anayetaka watu wajitoe kikamili[b] na hulipiza kisasi; Yehova analipiza kisasi[c] naye yuko tayari kuonyesha ghadhabu.[d] Yehova anawalipiza kisasi wapinzani wake,[e] naye ana kinyongo juu ya adui zake.[f]

3 Yehova si mwepesi wa hasira[g] naye ni mkuu katika nguvu,[h] wala hatasita kamwe kuadhibu.[i]

Njia yake imo katika upepo wenye kuharibu na katika dhoruba, na wingu kubwa ndilo mavumbi ya miguu yake.[j]

4 Anakemea bahari,[k] naye huikausha; huikausha mito yote.[l]

Bashani na Karmeli zimekauka,[m] na ua la Lebanoni limekauka.

5 Milima imetikisika kwa sababu yake, vilima navyo vikayeyuka.[n]

Dunia nayo itainuka kwa sababu ya uso wake; nchi yenye kuzaa pia, na wote wanaokaa ndani yake.[o]

6 Ni nani anayeweza kusimama mbele ya shutuma zake?[p] Ni nani anayeweza kusimama mbele ya joto la hasira yake?[q]

Ghadhabu yake mwenyewe itamwagwa kama moto,[r] nayo miamba itabomolewa kwa sababu yake.

7 Yehova ni mwema,[s] yeye ni ngome[t] katika siku ya taabu.[u]

Naye hutambua wale wanaotafuta kimbilio kwake.[a]

8 Ataangamiza kwa ukamili mahali pake kwa furiko linalopita,[b] na giza litawafuata adui zake.[c]

9 Mtatunga nini juu ya Yehova?[d] Yeye anasababisha maangamizi kamili.

Taabu haitazuka mara ya pili.[e]

10 Ijapokuwa wanasokotwa kama miiba[f] nao wamelewa kama kwa pombe yao ya ngano,[g] watamezwa kama majani yaliyokauka kabisa.[h]

11 Kwako atatoka yule anayetunga juu ya Yehova jambo lililo baya,[i] akitoa shauri lisilofaa.[j]

12 Yehova amesema hivi: "Ijapokuwa walikuwa katika hali kamili na wengi walikuwa katika hali hiyo, hata katika hali hiyo watakatwa;[k] na mmoja atapita kati. Nami nitakutesa, hivi kwamba nisikutese tena kamwe.[l] **13** Na sasa nitaivunja nira yake itoke juu yako,[m] na pingu zilizo juu yako nitazikata vipande viwili.[n] **14** Basi Yehova ameamuru hivi juu yako, 'Hakitapandwa chochote tena kamwe juu ya jina lako.[o] Nitakatilia mbali sanamu ya kuchongwa na sanamu ya kuyeyushwa kutoka katika nyumba ya miungu yako.[p] Nami nitakufanyia kaburi,[q] kwa sababu huna maana.'

SURA 1

a Isa 10:12
Nah 3:7
Sef 2:13
b Kut 20:5
Kum 4:24
Yos 24:19
c Kum 32:35
Mik 5:15
Ro 13:4
Ebr 10:30
d Isa 59:18
Yer 30:24
Ro 3:5
e Kum 32:41
Zb 81:14
Zb 97:3
f Mik 5:9
Ro 2:5
2Pe 2:9
g Hes 14:18
Yoe 2:13
h Ayu 9:4
Zb 62:11
Efe 1:19
i Kut 34:7
Yer 46:28
Amo 3:2
j Kut 19:18
Ayu 38:1
Zb 50:3
Zek 9:14
k Ayu 38:11
Zb 104:7
Zb 107:29
l Yos 3:16
Zb 74:15
Isa 19:5
m Isa 33:9
Amo 1:2
n 2Sa 22:8
Zb 68:8
Zb 97:5
Ebr 12:26
o Zb 97:4
Isa 24:1
p Yer 10:10
Ufu 6:17
q Kum 32:22
Ufu 16:1
r Ufu 16:8
s Zb 25:8
Zb 136:1
Mt 19:17
t Zb 18:2
Zb 91:2
Met 18:10
Isa 25:4
u Zb 46:1
Zb 50:15
Zb 91:15

Safu ya 2

a Zb 1:6
2Ti 2:19
b Isa 28:17
Eze 13:13
Da 9:26
c Isa 8:22
Yer 13:16
Sef 1:15
Yud 6
d Zb 2:1
Zb 21:11
Isa 8:10
e Isa 10:25
f Mik 7:4
g Ho 4:18
h Isa 9:19
Isa 33:11
Mal 4:1

i 2Fa 18:13; 2Fa 19:22; Isa 10:7; j 2Nya 32:16; k 2Fa 19:35; Isa 37:36; l Isa 60:18; Yoe 2:19; m Isa 14:25; Yer 30:8; Ho 11:4; n Zb 107:14; Yer 5:5; o Zb 109:13; Met 10:7; p Kut 34:13; q 2Nya 32:21.

15 "Tazama! Milimani, miguu ya mtu anayeleta habari
njema, anayetangaza amani.[a]
Ee Yuda, fanya sherehe zako.[b]
Timiza nadhiri zako;[c] kwa sa-
babu mtu yeyote asiyefaa kitu
hatapita tena kamwe katika-
ti yako.[d] Hatakosa kukatiliwa
mbali kabisa."[e]

2 Yule anayetawanya ame-
kuja mbele ya uso wako.[f]
Mahali penye ngome na pa-
lindwe. Ilinde njia. Vitie ngu-
vu viuno. Itegemeze nguvu
sana.[g]
2 Kwa maana Yehova ata-
kusanya fahari ya Yakobo,[h]
kama fahari ya Israeli, kwa
sababu wanaomaliza wamewa-
maliza.[i] Na machipukizi yao
wameyaharibu.[j]
3 Ngao ya wanaume wake
wenye uwezo imetiwa rangi
nyekundu; wanaume wake we-
nye nguvu wamevaa nguo za
rangi nyekundu.[k] Gari lake la
vita ni moto wa vifaa vya chu-
ma katika siku ya kujitayari-
sha kwake, na mikuki ya mbe-
roshi[l] imetikiswa. **4** Maga-
ri ya vita yanazidi kuende-
shwa kiwazimu barabarani.[m]
Yanakimbia-kimbia katika vi-
wanja vya watu wote. Kuone-
kana kwake ni kama mienge.
Kama umeme[n] yanakimbia-ki-
mbia.
5 Atawakumbuka watu wake
wenye fahari.[o] Watajikwaa wa-
napotembea.[p] Watafanya ha-
raka kwenda kwenye ukuta
wake, na kizuizi kitawekwa
imara. **6** Milango ya mito ita-
funguliwa, nalo jumba la mfa-
lme litayeyushwa. **7** Na ime-
amuliwa; amefunuliwa; atachu-
kuliwa,[q] na vijakazi wake wata-
omboleza, kama sauti ya
njiwa,[a] wakipiga-piga mioyo
yao.[b] **8** Ninawi naye, tangu
siku ambazo amekuwako,[c] ali-
kuwa kama kidimbwi cha maji;[d]
lakini wanakimbia. "Simameni
tuli! Simameni tuli!" Lakini ha-
kuna anayegeuka.[e]
9 Poreni fedha; poreni dha-
habu;[f] kwa maana hakuna ki-
komo cha vitu vilivyopangwa.
Kuna kiasi kikubwa cha na-
mna zote za vyombo vyenye
kutamanika.[g]
10 Utupu na uwazi, na jiji
lililofanywa ukiwa![h] Na moyo
unayeyuka,[i] magoti yanatete-
meka,[j] maumivu makali yamo
katika viuno vyote.[k] Na nyu-
so zao wote zimekuwa na wa-
siwasi.[l] **11** Liko wapi tundu
la simba, na pango la wana-si-
mba wenye manyoya shingo-
ni, ambamo simba alitembea
na kuingia,[m] ambamo mlikuwa-
mo mwana-simba, wala
hakuna mtu yeyote aliyeku-
wa akiwatetemesha?[n] **12** Si-
mba alikuwa akirarua-rarua
vipande vya kutosha kwa ajili
ya watoto wake, naye alikuwa
akinyonga kwa ajili ya simba-
jike wake. Naye alijaza daima
mawindo ndani ya matundu
yake na mahali pake pa kujifi-
cha alipajaza wanyama walio-
raruliwa vipande-vipande.[o]
13 "Tazama! Mimi niko dhi-
di yako," asema Yehova wa ma-
jeshi,[p] "nami nitaliteketeza
gari lake la vita katika moshi.[q]
Na upanga utawameza wana-
simba wako wenye manyoya
shingoni.[r] Nami nitakatilia
mbali mawindo yako kuto-
ka duniani, wala haitasikika
tena sauti ya wajumbe wako."[s]

SURA 1
a Isa 52:7
Lu 2:10
b Kum 16:16
Ne 10:33
c Zb 116:14
d Isa 52:1
e Zb 37:10
Zb 109:13
Mt 25:46

SURA 2
f Yer 25:9
Yer 49:32
Eze 29:12
g Yer 46:3
h Zb 47:4
Amo 8:7
i 2Fa 17:6
j Mwa 49:22
Ho 10:1
k Isa 63:3
l Isa 14:8
Zek 11:2
m Isa 37:24
Eze 26:10
n Hab 3:11
o Zb 136:18
Yer 50:29
p Yer 46:12
q Isa 20:4
Yer 29:1

Safu ya 2
a Isa 38:14
Isa 59:11
b Lu 23:27
c Mwa 10:11
d Ufu 17:15
e Yer 50:16
Sef 2:13
f Isa 33:1
Eze 26:12
g Ufu 18:12
h Isa 24:1
Sef 2:13
i Yos 2:11
Zb 22:14
Isa 13:7
j Da 5:6
k Isa 21:3
l Yoe 2:6
m Yer 2:15
Yer 50:17
n Isa 31:4
Sef 3:3
o Zb 17:12
p Isa 10:12
q Yos 11:9
Zb 46:9
r Isa 31:8
s 2Fa 18:17
2Fa 19:35

3 Ole wake jiji la umwagaji
wa damu.[a] Limejaa udanganyifu na unyang'anyi. Mawindo hayaondoki! **2** Kuna sauti ya mjeledi[b] na sauti ya mgongano wa gurudumu, na farasi anayetimua mbio na gari linalorukaruka.[c] **3** Mpandafarasi, na kumetameta kwa upanga, na kumetameta kwa mkuki,[d] na watu wengi waliouawa, na rundo kubwa la mizoga; wala hakuna mwisho wa maiti. Wanaendelea kujikwaa kati ya maiti zao; **4** kwa sababu ya wingi wa matendo ya ukahaba ya yule kahaba,[e] mwenye kupendeza kwa uvutio, mwanamke stadi wa ulozi, yeye anayeyanasa mataifa kwa matendo yake ya ukahaba na kuzinasa familia kwa ulozi wake.[f]

5 "Tazama! Mimi niko dhidi yako,"[g] asema Yehova wa majeshi, "nami nitaweka upindo wa marinda yako juu ya uso wako, nami nitayafanya mataifa yauone uchi wako,[h] na falme aibu yako. **6** Nami nitakutupia machukizo,[i] nitakufanya udharaulike; nami nitakuweka uwe tamasha.[j] **7** Ndipo itakuwa kwamba kila mtu anayekuona atakukimbia[k] naye atasema, 'Ninawi ameporwa! Ni nani atakayemsikitikia?' Nitakutafutia wapi wafariji? **8** Je, wewe ni bora kuliko No-amoni,[l] aliyekuwa akiketi kando ya mifereji ya Nile?[m] Maji yalimzunguka kotekote, mali yake ilikuwa bahari, ukuta wake ulikuwa bahari. **9** Ethiopia na Misri[n] pia walikuwa nguvu zake kamili; nazo hazikuwa na kikomo. Waputu na Walibya nao walikuwa msaada kwako.[a] **10** Yeye, pia, alikusudiwa uhamisho; alienda utekwani.[b] Watoto wake mwenyewe pia wakavunjwa vipande-vipande mbele ya barabara zote.[c] Wakapiga kura[d] juu ya watu wake waliotukuzwa, na wakuu wake wote wamefungwa kwa pingu.[e]

11 "Wewe mwenyewe utalewa pia;[f] utakuwa kitu kilichofichika.[g] Wewe mwenyewe pia utatafuta ngome ya kujikinga kutoka kwa adui.[h] **12** Mahali pako pote penye ngome ni kama mitini iliyo na matunda ya kwanza yaliyoiva, ambayo, ikitikiswa-tikiswa, yataanguka katika kinywa cha mwenye kula.[i]

13 "Tazama! Watu wako ni wanawake katikati yako.[j] Bila shaka malango ya nchi yako yatafunguliwa adui zako. Moto utateketeza mapingo yako.[k] **14** Jitekee maji kwa ajili ya kuzingirwa.[l] Tia nguvu mahali pako penye ngome.[m] Ingia matopeni, kanyaga-kanyaga udongoni; kamata kalibu ya matofali. **15** Hata huko utateketezwa na moto. Upanga utakukatilia mbali.[n] Nawe utaliwa na upanga kama nzige[o] wachanga wanavyokula. Jifanye kuwa hesabu kubwa kama nzige wachanga; jifanye kuwa hesabu kubwa kama nzige. **16** Umezidisha wafanya-biashara wako kuliko nyota za mbinguni.[p]

"Nzige mchanga naye, huvua ngozi yake; kisha huruka mbali. **17** Walinzi wako ni kama nzige, na maofisa wako wa uandikishaji ni kama kundi la nzige. Wanapiga kambi

SURA 3

a Hab 2:12
b Met 26:3
c Amu 5:22
Yer 47:3
d Hab 3:11
e Isa 23:17
Eze 23:30
f Law 19:26
Kum 18:10
1Ko 10:20
g Nah 2:13
h Isa 47:2
Yer 13:22
Eze 16:37
Ufu 17:16
i Mal 2:3
j Sef 2:15
Yud 7
k Nah 2:8
l Yer 46:25
Eze 30:14
m Isa 19:6
n Isa 20:5

Safu ya 2

a Mwa 10:6
2Nya 16:8
Yer 46:9
Eze 27:10
b Zb 33:16
Isa 20:4
c Zb 137:9
Isa 13:16
d Yoe 3:3
Oba 11
e Zb 149:8
f Zb 75:8
Yer 25:15
g Yos 10:16
1Sa 13:6
h Yer 4:5
i Isa 28:4
Ufu 6:13
j Isa 19:16
Yer 51:30
k Zb 107:16
Isa 45:2
l 2Nya 32:3
2Nya 32:4
m Isa 8:9
Yoe 3:9
n Sef 2:13
o Kut 10:14
Yoe 1:4
p Mwa 15:5
Yer 33:22

katika mazizi ya mawe siku yenye baridi. Lazima jua liangaze, nao huruka mbali; na mahali pao hapajulikani.[a]

18 "Wachungaji wako wamesinzia,[b] Ee mfalme wa Ashuru; wenye fahari wako wanakaa katika makao yao.[c] Watu wako wametawanywa juu ya milima, wala hakuna anayewakusanya pamoja.[a] **19** Hakuna kitulizo cha msiba wako. Pigo lako haliponyeki.[b] Wote wanaosikia habari juu yako wewe watakupigia makofi;[c] kwa sababu ni nani ambaye ubaya wako haukupita daima juu yake?"[d]

SURA 3
a Zb 109:23
b Zb 76:5; Isa 56:10; Yer 51:39
c Yer 51:30

Safu ya 2
a 1Fa 22:17; Nah 2:8; Ufu 6:15
b Yer 46:11; Eze 30:21; c Ayu 27:23; Sef 2:15; d Isa 10:6; Isa 37:18.

HABAKUKI

1 Tangazo ambalo Habakuki nabii aliona katika maono: **2** Ee Yehova, nililie msaada mpaka wakati gani, nawe usisikie?[a] Nitakuomba msaada kutokana na jeuri mpaka wakati gani, nawe usiokoe?[b] **3** Kwa nini unanionyesha jambo lenye kudhuru, nawe unaendelea kutazama taabu tupu? Na kwa nini kuna uporaji na jeuri mbele yangu, kwa nini kugombana hutokea, kwa nini mzozo huendelezwa?[c]

4 Basi sheria hufa ganzi, na haki haitendeki kamwe.[d] Kwa kuwa mwovu anamzingira mwadilifu, kwa sababu hiyo haki hupotoshwa.[e]

5 "Oneni, kati ya mataifa, tazameni, mkaangaliane kwa mshangao.[f] Shangaeni; kwa maana kuna utendaji ambao mtu anaufanya katika siku zenu, ambao hamtaamini ijapokuwa unasimuliwa.[g] **6** Kwa maana, tazama, ninawasimamisha Wakaldayo,[h] taifa lenye uchungu na lenye haraka, linaloenda kote duniani ili kumiliki makao yasiyo yake.[i] **7** Taifa hilo ni lenye kutisha na lenye kuogopesha. Haki na utukufu wake hutoka ndani yake.[a] **8** Na farasi zake ni wepesi kuliko chui, nao ni wakali kuliko mbwa-mwitu wa jioni.[b] Na farasi zake wa vita wamekanyaga udongo, na hao farasi zake huja kutoka mbali. Linaruka kama tai anayeharakisha kwenda kula kitu.[c] **9** Lote huja ili kufanya jeuri tupu.[d] Kukusanywa kwa nyuso zao ni kama upepo wa mashariki,[e] nalo linakusanya mateka kama vile mchanga. **10** Nalo linawadhihaki wafalme, nalo linawacheka maofisa wakuu.[f] Hata kila mahali penye ngome linapacheka,[g] nalo linarundika mavumbi na kupateka. **11** Wakati huo litasonga mbele kama upepo, litapita kati na kuwa na hatia.[h] Nguvu zake zinatokana na mungu wake."[i]

12 Je, wewe si wa tangu zamani za kale, Ee Yehova?[j] Ee Mungu wangu, Mtakatifu wangu, wewe hufi.[k] Ee Yehova,

SURA 1
a Zb 13:1; Ufu 6:10
b Zb 22:1; Zb 74:10; Mhu 5:8
c Mhu 4:1; Ro 9:22; 2Pe 2:8; 2Pe 3:9
d Ayu 12:6; Zb 12:8; Mhu 8:11; Mt 23:23
e Ayu 33:27; Met 29:2; Isa 1:21; Mt 26:59; Mdo 7:52
f Omb 4:12
g Isa 28:21; Isa 29:14; Mdo 13:41
h Yer 22:7; Yer 46:2
i Kum 28:49; Yer 5:15; Yer 6:22; Eze 23:23

Safu ya 2
a Yer 39:5; Yer 52:9; Da 5:19
b Yer 5:6
c Yer 4:13; Omb 4:19; Eze 17:3
d Kum 28:51; Yer 25:9
e Isa 27:8; Eze 17:10
f 2Fa 24:12; 2Nya 36:17
g Yer 32:24; Yer 52:7
h Isa 47:6; Yer 51:24; Zek 1:15
i Da 5:4
j Zb 90:2; Zb 93:2; Ufu 1:8
k 1Ti 1:17; Ufu 15:3.

umeliweka kwa ajili ya hukumu; na kwa ajili ya kukaripia[a]
umeliwekea msingi, Ee Mwamba.[b]
13 Wewe umetakata sana
usiweze kuona lililo baya; nawe
huwezi kuitazama taabu.[c] Kwa
nini unawatazama wale wanaotenda kwa hila,[d] na kukaa kimya wakati mtu mwovu anapommeza mtu aliye mwadilifu
kuliko yeye?[e] **14** Na kwa nini
unamfanya mtu wa udongo
kuwa kama samaki wa baharini, kama vitu vinavyotambaa
ambavyo havina mtawala?[f]
15 Hao wote amewainua kwa
ndoano tu;[g] huwakokota katika wavu wake,[h] naye huwa-
kusanya katika wavu wake
wa kuvulia. Hiyo ndiyo sababu anafurahi na kuwa na shangwe.[i] **16** Ndiyo sababu yeye
huutolea dhabihu wavu wake
wa kukokota na kuufukizia
wavu wake wa kuvulia moshi wa dhabihu; kwa maana
kwa vitu hivyo fungu lake limetiwa mafuta ya kutosha, na
chakula chake ni chenye afya.[j]
17 Je, hiyo ndiyo sababu atamwaga vyote vilivyomo katika wavu wake wa kukokota,
na je, anapaswa kuyaua mataifa daima, bila kuonyesha huruma?[k]

2 Nitaendelea kusimama katika kituo changu cha ulinzi,[l] nitaendelea kusimama
juu ya boma; nitaendelea kuangalia,[m] ili kuona atakaloniambia[n] na lile nitakalojibu nikikaripiwa.[o]
2 Yehova naye akanijibu na
kusema: "Andika maono hayo,
na kuyaweka waziwazi kwenye mabamba,[p] ili anayeyasoma kwa sauti aweze kufanya
hivyo kwa wepesi.[a] **3** Kwa
maana maono hayo bado ni ya
wakati uliowekwa,[b] nayo yanafanya haraka kuelekea mwisho, wala hayatasema uwongo.
Hata yakikawia, endelea kuyatarajia; kwa maana bila shaka
yatatimia.[c] Hayatachelewa.
4 "Tazama! Nafsi yake imejivuna;[d] haikuwa nyoofu ndani yake. Lakini mwadilifu, ataendelea kuishi kwa uaminifu
wake.[e] **5** Na, kwa kweli, kwa
sababu divai inatenda kwa
hila,[f] mwanamume anajidai;[g]
naye hatafikia mradi wake,[h]
yeye ambaye ameifanya nafsi
yake iwe na nafasi kubwa
kama Kaburi,* na aliye kama
kifo, asiyeweza kutoshelezwa.[i]
Naye huendelea kujikusanyia
kwake mataifa yote na kujikusanyia kwake vikundi vyote
vya watu.[j] **6** Je, hawa wote
hawatamtungia neno la kimethali[k] na maelezo ya kudokeza,
mafumbo juu yake? Na mtu
atasema,
"'Ole wake anayezidisha kisicho chake[l]—Ee mpaka wakati gani![m]—na yule anayefanya deni lake mwenyewe liwe
zito! **7** Je, wale wanaodai fa-
ida kwako hawatasimama ghafula, na wale wanaokutikisa
kwa jeuri waamke, nawe uwe
kwao kitu cha kunyakuliwa?[n]
8 Kwa sababu wewe mwenye-
we uliyapora mataifa mengi,
mabaki yote ya vikundi vya
watu watakupora,[o] kwa saba-
bu ya kumwaga damu ya wanadamu na kwa sababu ya dunia kufanyiwa jeuri, mji na
wale wote wanaokaa ndani
yake.[p]

SURA 1
a Yer 10:24 Yer 30:11 Ebr 12:5
b Kum 32:4 1Sa 2:2 Zb 18:2
c Zb 5:4 Isa 59:2 1Pe 1:15
d Yer 12:1
e Zb 35:22 Zb 37:14 Zb 50:21
f Met 6:7 Isa 63:19
g Mhu 9:12
h Zb 10:9 Mik 7:2
i Yer 50:11
j Kum 8:17 Zb 37:1
k 2Nya 36:17 Nah 3:7

SURA 2
l Mik 7:7
m Isa 21:8 Isa 62:6
n Zb 85:8 2Ko 13:3 Ebr 1:1
o Ayu 23:5
p Kut 17:14 Kum 27:8

Safu ya 2
a Kum 31:11 Ne 8:8
b Da 8:19 Da 10:14 Mdo 17:26
c Mik 7:7 Yak 5:7
d Da 5:20 Lu 18:14
e Yoh 3:36 Ro 1:17 Ga 3:11 Ebr 10:38
f Met 20:1
g 2Fa 14:10 Met 21:24
h Met 11:2 Met 16:18
i Met 27:20 Mhu 5:10
j Isa 14:17
k Isa 14:4 Mik 2:4
l Met 22:16 Yak 5:4
m Zb 94:3
n Met 29:1 Yer 51:11
o Isa 13:19 Isa 33:1 Yer 27:7 Zek 2:9
p 2Nya 36:17 Zb 137:8 Ufu 6:10

Hab 2:5* Sheoli. Tazama Nyongeza 4.

9 "'Ole wake anayeipatia
nyumba yake faida ya uovu,[a]
ili kukiweka kiota chake kileleni, ili kukombolewa kutoka mkononi mwa jambo lenye
msiba!b **10** Umeshauri jambo
la aibu kwa nyumba yako, kukatiliwa mbali kwa vikundi vingi vya watu;[c] na nafsi yako
inafanya dhambi.[d] **11** Kwa
maana jiwe litalia kwa huzuni
kutoka ukutani, na boriti litalijibu kutoka kati ya mbao za
paa.[e]

12 "'Ole wake anayejenga
jiji kwa umwagaji wa damu,
anayesimamisha imara mji
kwa ukosefu wa uadilifu!f
13 Tazama! Je, si kutoka kwa
Yehova wa majeshi kwamba vikundi vya watu vitaendelea
kufanya kazi ya taabu kwa ajili ya moto tu, na kwamba vikundi vya mataifa vitajichosha
bure tu?g **14** Kwa maana dunia itajawa na kuujua utukufu
wa Yehova kama maji yanavyoifunika bahari.[h]

15 "'Ole wake anayewapa
wenzake kinywaji, akikishikamanisha na ghadhabu na hasira yako, ili kuwalewesha,[i] kwa
kusudi la kuzitazama sehemu zao za aibu.[j] **16** Utashibishwa kwa aibu badala ya utukufu.[k] Kunywa pia, wewe
mwenyewe,[l] ukaonwe kuwa
mtu ambaye hajatahiriwa.[m]
Kikombe cha mkono wa kuume wa Yehova kitakufikia,[n] na
kutakuwako fedheha juu ya
utukufu wako; **17** kwa sababu jeuri iliyofanywa juu ya Lebanoni[o] ndiyo itakayokufunika, na tamaa juu ya wanyama
wanaowaogopesha, kwa sababu ya kumwaga damu ya wanadamu na jeuri iliyofanywa dunia,[a] ule mji na wale
wote wanaokaa ndani yake.[b]
18 Sanamu ya kuchongwa
imekuwa na faida gani,[c] wakati yeye aliyeifanya ameichonga, sanamu ya kuyeyushwa,
na mfundishaji wa uwongo?[d]
wakati yeye aliyefanya umbo
lake ameitegemea,[e] kufikia hatua ya kufanya miungu isiyo
na thamani ambayo haiwezi
kusema?[f]

19 "'Ole wake anayekiambia
kipande cha mti: "Ee amka!"
anayeliambia jiwe lisiloweza kusema: "Ee amka! Hizo zenyewe
zitafundisha"?g Tazama! Zimefunikwa kwa dhahabu na fedha,[h]
wala hamna pumzi yoyote katikati yake.[i] **20** Lakini Yehova yumo katika hekalu lake takatifu.[j] Kaa kimya mbele zake,
dunia yote!'"[k]

3 Sala ya Habakuki nabii katika nyimbo za huzuni:
2 Ee Yehova, nimeisikia habari juu yako.[l] Nimeogopa utendaji wako,[m] Ee Yehova.

Ufanye hai utendaji wako
katikati ya ile miaka! Ufanye
ujulikane katikati ya ile miaka. Wakati wa msukosuko, ukumbuke kuonyesha rehema.[n]

3 Mungu mwenyewe alikuja kutoka Temani, Mtakatifu
kutoka Mlima Parani.[o] *Sela*.[p]

Utukufu wake ulizifunika
mbingu;[q] na dunia ikajazwa
sifa yake.[r]

4 Nao uangavu wake, ukawa kama vile nuru.[s] Alikuwa
na miale miwili ikitoka mko-

SURA 2
a 1Fa 21:2; Yer 22:13
b Zb 49:11; Met 18:11; Oba 4
c Isa 14:20
d Hes 16:38; 1Fa 2:23; Met 8:36; Eze 18:20
e Mwa 4:10; Yak 5:4
f Yer 22:13; Eze 24:9; Nah 3:1; Ufu 17:6
g Met 21:30; Isa 50:11; Yer 51:58
h Zb 72:19; Isa 11:9; Zek 14:9
i 2Sa 11:13; 2Sa 13:28; Ufu 17:2; Ufu 18:3
j Mwa 9:22; Eze 22:10
k Flp 3:19
l Zb 75:8; Isa 51:22; Yer 51:57; Ufu 18:6
m Eze 28:10; Eze 32:19
n Yer 25:28
o Zek 11:1

Safu ya 2
a Zb 137:8; Met 28:17; Ufu 18:24
b Yer 50:28; Yer 51:24
c Isa 37:38; Isa 42:17; Yer 2:28; 1Ko 8:4
d Yon 2:8; Zek 10:2; Ro 1:21
e Zb 115:8; Isa 44:19; Isa 45:20
f Yer 10:5; 1Ko 12:2
g Zb 97:7; Isa 37:19; Da 3:29
h Isa 40:19; Isa 46:6; Mdo 17:29; Mdo 19:24
i Zb 135:17; Yer 10:14; Yer 51:17
j Zb 11:4; Zb 115:3; Isa 6:1; Ebr 8:2
k Zb 76:8; Sef 1:7; Zek 2:13

SURA 3 l Zb 145:11; Isa 53:1; m Zb 64:9; n Kut 32:13; Yer 31:20; Omb 3:32; Mt 24:22; o Kum 33:2; Amu 5:4; p Zb 68:7; q Kut 19:16; Zb 18:13; Ebr 12:18; r Zb 148:13; Isa 6:3; s Kut 13:21; Zb 104:2; Isa 60:20; Ufu 22:5.

noni mwake, na hapo ndipo palipofichwa nguvu zake.[a]

5 Tauni ikaenda mbele zake,[b] na homa kali ilikuwa ikitoka miguuni pake.[c]

6 Alisimama tuli, apate kuitikisa dunia.[d] Aliona, kisha akayarusha mataifa.[e]

Na milima ya milele ikavunjwa;[f] vilima vinavyodumu kwa wakati usio na kipimo vikainama.[g] Miendo ya zamani za kale ni yake.

7 Chini ya kitu chenye kudhuru niliona mahema ya Kushani. Vitambaa vya mahema ya nchi ya Midiani[h] vikaanza kufadhaika.[i]

8 Je, ni juu ya mito, Ee Yehova, je, hasira yako imewaka juu ya mito,[j] au je, ghadhabu yako iko juu ya bahari?[k] Kwa maana ulipanda farasi zako;[l] magari yako yalikuwa wokovu.[m]

9 Katika uchi wake upinde wako hufunuliwa.[n] Viapo rasmi vya makabila ndivyo jambo lililosemwa.[o] *Sela*. Ukaipasua dunia kwa mito.[p]

10 Milima ilikuona; ikawa katika maumivu makali.[q] Dhoruba ya maji yenye mngurumo ikapita kati. Kilindi cha maji kikatoa mvumo wake.[r] Kikainua mikono yake juu.

11 Jua—mwezi—vilisimama tuli,[s] kwenye makao yaliyo juu sana.[t] Kama nuru mishale yako mwenyewe ikaenda mfululizo.[u] Mng'ao wa mkuki wako ukaangaza.[v]

12 Kwa shutuma ulipiga mwendo kati ya dunia. Kwa hasira ukayapura mataifa.[w]

13 Ukajitokeza kwa ajili ya wokovu wa watu wako,[x] upate kumwokoa mtiwa-mafuta wako. Ulimvunja vipande-vipande aliye kichwa kutoka kwa nyumba ya mwovu.[a] Msingi uliwekwa wazi, mpaka shingoni.[b] *Sela*.

14 Kwa fimbo zake mwenyewe ulikichoma[c] kichwa cha mashujaa wake wa vita waliposonga kama tufani ili kunitawanya.[d] Upeo wao wa raha ulikuwa kama wa wale wanaokusudia kummeza mwenye kuteseka katika maficho.[e]

15 Kupitia bahari ulikanyaga kwa farasi zako, kupitia mkusanyo wa maji mengi.[f]

16 Nilisikia, tumbo langu likaanza kutetemeka; midomo yangu ilitetemeka kwa sababu ya ule mvumo; kuoza kukaanza kuingia katika mifupa yangu;[g] na katika hali yangu nikafadhaika, kwamba ningojee kimya siku ya taabu,[h] kuja kwake kwa watu,[i] apate kuwavamia.

17 Ijapokuwa huenda mtini usichanue,[j] kusiwe na mazao kwenye mizabibu; kazi ya mzituni ikashindwa, matuta yasizae chakula chochote.[k] Huenda kundi liondolewe zizini, na kusiwe na mifugo katika mazizi;[l]

18 Lakini mimi, nitafurahi katika Yehova mwenyewe;[m] nitakuwa na shangwe katika Mungu wa wokovu wangu.[n]

pia litakuwa na maumivu ma-
kali sana; Ekroni[l] pia, kwa sa-
babu tumaini lake analotaza-
mia[m] litaona aibu. Na mfalme
ataangamizwa kutoka Gaza,
nalo Ashkeloni halitakaliwa
na watu.[n] **6** Na mwana-ha-
ramu[o] ataketi huko Ashdo-
di,[p] nami nitakikatilia mbali
kiburi cha Mfilisti.[q] **7** Nami
nitaviondoa vitu vyake vye-
nye madoa ya damu kinywa-
ni mwake na kuyaondoa ma-
chukizo yake kutoka katikati
ya meno[r] yake, naye mwenye-
we atabaki kwa ajili ya Mu-
ngu wetu; naye atakuwa kama
shehe[s] katika Yuda,[t] na Ekroni
kama Myebusi.[u] **8** Nami ni-
tapiga kambi kama mlinzi wa
mbele kwa ajili ya nyumba ya-

SURA 8
a Law 19:11; Met 12:19; Yer 9:5; Efe 4:15; Efe 4:25
b Isa 11:4; Amo 5:15; Zek 7:9
c Met 3:29; Yer 4:14; Zek 7:10; Mt 15:19
d Yer 4:2; Zek 5:4
e Met 6:16; Met 8:13
f Yer 52:6
g Yer 52:12; Zek 7:5
h 2Fa 25:25
i Yer 52:4
j Zb 30:11; Isa 35:10; Yer 31:12
k Zb 119:165
l Zb 22:27; Isa 2:2; Isa 11:10; Ho 1:10; Mt 8:11
m Zb 122:1
n Zek 7:2
o Yer 50:4
p Isa 55:5; Isa 60:3; Mik 4:2; Hag 2:7; Ga 3:8
q Ufu 7:9; Ufu 14:6
r Mt 25:40
s Ro 2:29; Ga 3:29
t Kut 12:38; Hes 10:29; Ru 1:16; Mdo 13:47

Safu ya 2
a Kum 4:7; Isa 45:14; 1Ko 14:25

SURA 9
b Isa 13:1
c Yer 49:27; Amo 1:3
d 2Nya 16:9; Ebr 4:13; 1Pe 3:12
e Yer 49:23; Amo 6:14
f Isa 23:1; Yoe 3:4; Amo 1:9
g Eze 28:21
h Eze 28:3
i Eze 27:33
j Eze 26:17; Eze 27:26
k Eze 28:18
l Yos 13:3; 1Sa 5:10
m Isa 20:5
n Sef 2:4
o Kum 23:2; Ebr 12:8
p Mhu 2:18; Amo 1:8

q Isa 2:17; Da 4:37; r Zb 58:6; Amo 3:12; s Mwa 36:40; t Isa 60:14; u 2Sa 5:6; 1Fa 9:20; 1Nya 11:4; 1Nya 21:28.

ngu,[a] ili kusiwe na mtu yeyote anayepita kati wala anayerudi; wala msimamizi wa kazi[b] hatapita tena kwao, kwa maana sasa nimeyaona kwa macho yangu.[c]

9 "Shangilia sana, Ee binti Sayuni.[d] Piga kelele za ushindi,[e] Ee binti Yerusalemu. Tazama! mfalme[f] wako anakuja kwako.[g] Yeye ni mwadilifu, ndiyo, ameokolewa;[h] ni mnyenyekevu,[i] naye amepanda juu ya punda, juu ya mnyama mkomavu, mwana wa punda-jike.[j] **10** Nami nitalikatilia mbali gari la vita kutoka katika Efraimu na farasi kutoka katika Yerusalemu.[k] Na upinde wa mapigano[l] utakatiliwa mbali. Naye atasema amani kwa mataifa;[m] na utawala wake utakuwa kutoka bahari mpaka bahari na kutoka Mto mpaka mipaka ya dunia.[n]

11 "Nawe pia, Ee mwanamke, nitawatoa wafungwa[o] wako kutoka katika shimo ambalo halina maji kwa kutumia damu ya agano[p] lako.

12 "Rudini katika ngome,[q] enyi wafungwa wa lile tumaini.[r]

"Pia, leo ninakuambia, 'Nitakulipa fungu lililo mara mbili,[s] Ee mwanamke. **13** Kwa maana nitamkanyaga Yuda kama upinde wangu. Nami nitamtia Efraimu katika upinde, nami nitawaamsha wana wako, Ee Sayuni, kupigana na wana wako,[t] Ee Ugiriki,[u] nami nitakufanya kama upanga wa mwanamume mwenye nguvu.'[v] **14** Na Yehova mwenyewe ataonekana juu yao,[w] na mshale wake utaenda kama umeme.[a] Naye Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova atapiga baragumu,[b] ataenda pamoja na dhoruba za upepo wa kusini.[c] **15** Yehova wa majeshi mwenyewe atawalinda wao, nao watakula[d] na kuyatiisha mawe ya kombeo. Nao watakunywa[e]—wafanye kelele—kana kwamba kuna divai; nao watajazwa kama bakuli, kama pembe za madhabahu.[f]

16 "Na Yehova Mungu wao atawaokoa[g] katika siku hiyo kama kundi la watu wake;[h] kwa maana watakuwa kama mawe ya taji yanayong'aa juu ya nchi yake.[i] **17** Kwa maana lo! jinsi ulivyo mkuu wema wake,[j] na jinsi ulivyo mkuu uzuri wake![k] Nafaka ndiyo itakayowasitawisha vijana, na divai mpya nayo itawasitawisha mabikira."[l]

10 "Mwombeni Yehova mvua[m] wakati wa mvua ya masika,[n] Yehova anayefanya mawingu ya dhoruba,[o] ambaye huwapa mvua kubwa,[p] na kumpa kila mmoja mimea shambani.[q] **2** Kwa maana terafimu[r] zimesema mambo ya uchawi; nao waaguzi wameona maono ya uwongo,[s] nao huendelea kusema ndoto za bure, nao hujaribu kufariji kwa ubatili.[t] Ndiyo sababu wataondoka kama kundi;[u] watateseka, kwa sababu hakuna mchungaji.[v]

3 "Hasira yangu imewaka juu ya wachungaji,[w] nami nitawatoza hesabu[x] viongozi walio

SURA 9

a Zb 125:2
b Isa 54:14
c Kut 3:7; 2Sa 16:12
d Isa 12:6
e Isa 44:23; Sef 3:14
f Zb 2:6; Isa 32:1; Yer 23:5; Lu 19:38; Yoh 1:49
g Yoh 12:15
h Yoh 16:33
i Mt 11:29; Mt 21:5
j IFa 1:33; Mt 21:7
k Met 21:31
l Zek 10:4
m Isa 9:7; Efe 2:14
n Kut 23:31; Zb 2:8; Zb 72:8
o Isa 49:9
p Yer 31:31; Mt 26:28; Ebr 12:24; Ebr 13:20; 1Pe 1:19
q 2Sa 5:7; Yer 31:6
r Isa 61:1; Yer 31:17
s Ayu 42:10; Isa 61:7
t Mt 13:38
u Da 8:21; Yoe 3:6
v Zb 149:6; Isa 41:15
w Kut 14:24

Safu ya 2

a Zb 18:14; Isa 18:3
b Yos 6:5
c Isa 21:1; Isa 66:15
d Mik 5:9; Zek 10:5; Zek 12:6
e Isa 55:1
f Kut 27:2; Law 4:7
g Eze 34:22; Eze 37:23
h Zb 100:3; Mik 5:4; Zek 11:7; Lu 12:32
i Isa 62:3; Sef 3:20
j Zb 25:8; Zb 31:19; Isa 63:7
k Zb 50:2; Zb 90:17
l Isa 62:8; Yoe 3:18; Amo 9:13

SURA 10

m Yer 14:22; Yak 5:18
n Kum 11:14; Yoe 2:23
o Yer 51:16
p Eze 34:26; Yak 5:7

q Zb 104:14; r 1Sa 15:23; s Yer 27:9; Yer 29:21; t Yer 8:11; u Yer 50:17; v Hes 27:17; Eze 34:5; w Isa 56:11; Yer 10:21; Eze 34:10; x Mk 12:40.

kama mbuzi;[a] kwa maana Yehova wa majeshi ameelekeza fikira zake kwa kundi lake,[b] nyumba ya Yuda, naye amewafanya kama farasi[c] wake mwenye heshima katika mapigano.
4 Kutoka kwake kuna mkuu,[d] kutoka kwake kuna mtawala anayetegemeza,[e] kutoka kwake kuna upinde wa mapigano;[f] kwake hutoka kila msimamizi wa kazi,[g] wote pamoja. **5** Nao watakuwa kama wanaume wenye nguvu[h] wanaokanyaga matope ya barabarani katika mapigano.[i] Nao watajihusisha katika mapigano, kwa maana Yehova yupo pamoja nao;[j] na hao wapanda-farasi wataona aibu.[k]
6 Nami nitaifanya nyumba ya Yuda iwe kuu, nami nitaiokoa nyumba ya Yosefu.[l] Nami nitawapa makao, kwa maana nitawaonyesha rehema;[m] nao watakuwa kama watu ambao sikutupilia mbali;[n] kwa maana mimi ni Yehova Mungu wao, nami nitawajibu.[o] **7** Na wale wa Efraimu watakuwa kama mwanamume mwenye nguvu,[p] na moyo wao utashangilia kana kwamba kutokana na divai.[q] Na wana wao wenyewe wataona nao hakika washangilie;[r] moyo wao utashangilia katika Yehova.[s]

8 "'Nitawapigia mluzi[t] na kuwakusanya pamoja; kwa maana nitawakomboa,[u] nao watakuwa wengi, kama wale ambao wamekuwa wengi.[v]
9 Nami nitawatawanya kama mbegu katikati ya mataifa,[w] nao watanikumbuka wakiwa mbali;[x] nao wataamka pamoja na wana wao na kurudi.[y]
10 Nami nitawarudisha kutoka nchi ya Misri;[a] nitawakusanya pamoja kutoka Ashuru;[b] nami nitawaleta katika nchi ya Gileadi[c] na Lebanoni, wala nafasi haitapatikana kwa ajili yao.[d] **11** Naye atapita baharini kwa taabu;[e] na ndani ya bahari atayapiga mawimbi,[f] na vilindi vyote vya Nile vitakauka.[g] Nacho kiburi cha Ashuru kitashushwa,[h] na fimbo ya enzi[i] ya Misri itaondoka.[j] **12** Nami nitawafanya wawe wakuu katika Yehova,[k] nao watatembea huku na huku katika jina lake,"[l] asema Yehova."

11 "Fungua milango yako, Ee Lebanoni,[m] ili moto uteketeze kati ya mierezi yako.[n]
2 Piga mayowe, Ee mberoshi, kwa maana mwerezi umeanguka; kwa sababu wenye utukufu wameporwa![o] Pigeni mayowe, enyi miti mikubwa sana ya Bashani, kwa maana msitu usiopenyeka umeanguka![p]
3 Sikiliza! Mayowe ya wachungaji,[q] kwa maana utukufu wao umeporwa.[r] Sikiliza! Kunguruma kwa wana-simba wenye manyoya shingoni, kwa maana vichaka vyenye kiburi kando ya Yordani vimeporwa.[s]

4 "Yehova Mungu wangu asema hivi, 'Chunga kundi lililokusudiwa kuuawa,[t] **5** ambalo wanunuzi wake huwaua[u] ingawa hawahesabiwi hatia.[v] Na wale wanaowauza[w] husema: "Yehova abarikiwe, huku nami nitapata utajiri."[x] Na wachungaji wao wenyewe hawawaonyeshi huruma yoyote.'[y]

SURA 10
a Eze 34:16; Eze 34:17
b Lu 1:68
c Met 21:31
d Isa 19:13; Hag 2:23
e Mwa 49:10; Ezr 9:8
f Mwa 49:24; Isa 49:2
g Isa 60:17
h Yoe 2:7
i Zb 18:42; Mik 7:10
j Kum 20:1; Isa 41:13
k Zb 20:7; Zb 33:16; Hag 2:22
l Yer 3:18; Eze 37:16; Ho 1:10
m Yer 31:20
n Yer 30:18
o Yer 33:3
p Yer 31:9; Eze 37:19
q Zb 104:15; Zek 9:15
r Zb 90:16; Yer 32:39
s Isa 66:14; Sef 3:14
t Ezr 1:1
u Isa 44:22; Isa 51:11; 1Ti 2:6
v 1Fa 4:20; Yer 33:22
w Yer 31:27; Ho 2:23; Mik 5:7; Mdo 8:4
x 1Fa 8:47; Yer 51:50
y Isa 65:23; Mdo 2:39

Safu ya 2
a Isa 11:11
b Yer 50:19; Ro 11:25
c Mik 7:14
d Isa 49:20; Isa 54:2
e Zb 66:12
f Isa 11:15
g Isa 19:6
h Isa 14:25; Mik 5:5
i Isa 19:1
j Eze 30:13
k Isa 41:10; Isa 45:24
l Met 18:10; Mik 4:5

SURA 11
m Yer 22:23
n Yer 22:7
o Isa 10:33; Eze 31:3
p Isa 2:13; Isa 32:19
q Eze 34:10; Yoe 1:13
r Yer 2:30
s Yer 49:19; Yer 50:44
t Eze 34:8
u Yer 23:1; Eze 22:25; Eze 34:2; Mik 3:2;
v Yer 2:3;
w 2Fa 4:1; Ne 5:8;
x Ho 12:8;
y Eze 34:4.

6 “‘Kwa maana sitawahurumia tena wakaaji wa nchi,’[a] asema Yehova. ‘Kwa hiyo nawafanya wanadamu wajikute, kila mmoja katika mkono wa mwenzake[b] na katika mkono wa mfalme[c] wake; nao wataivunja nchi vipande-vipande, nami sitakomboa kwa vyovyote kutoka mkononi mwao.’”[d]

7 Nami nililichunga kundi[e] lililokusudiwa kuuawa,[f] kwa ajili yenu, enyi wenye kuteseka wa kundi.[g] Kwa hiyo nikajichukulia fimbo[h] mbili. Moja nikaiita Uzuri,[i] na ile nyingine nikaiita Muungano,[j] nami nikaanza kulichunga kundi. **8** Mwishowe nikafutilia mbali wachungaji watatu katika mwezi mmoja,[k] kwa vile nafsi yangu ilikosa subira[l] kwao hatua kwa hatua, na pia nafsi zao zilinichukia. **9** Mwishowe nikasema: “Sitaendelea kuwachunga ninyi.[m] Yule anayekufa, na afe. Na yule anayefutiliwa mbali, na afutiliwe mbali.[n] Na wale waliobaki, kila mmoja na ale nyama ya mwenzake.”[o] **10** Basi nikachukua fimbo yangu inayoitwa Uzuri[p] na kuikata vipande-vipande,[q] ili kulivunja agano langu ambalo nilikuwa nimefanya pamoja na vikundi vyote vya watu.[r] **11** Nalo likavunjwa siku hiyo, na hivyo wenye kuteseka wa kundi[s] waliokuwa wakinitazama[t] wakajua kwamba hilo lilikuwa neno la Yehova.

12 Ndipo nikawaambia: “Ikiwa vema machoni penu,[u] nipeni mshahara wangu; lakini kama sivyo, acheni.” Basi wakalipa mshahara wangu, vipande 30 vya fedha.[v]

13 Kwa hiyo Yehova akaniambia: “Utupe ndani ya hazina[a]—thamani tukufu ambayo nimekadiriwa kwa maoni yao.”[b] Ndipo nikavichukua vile vipande 30 vya fedha, nami nikavitupa ndani ya hazina katika nyumba ya Yehova.[c]

14 Kisha nikaikata vipande-vipande fimbo yangu ya pili, inayoitwa Muungano,[d] ili kuuvunja undugu[e] kati ya Yuda na Israeli.[f]

15 Kisha Yehova akaendelea kuniambia: “Jichukulie tena vifaa vya mchungaji asiyefaa kitu.[g] **16** Kwa maana tazama, ninamwacha mchungaji asimame katika nchi hii.[h] Hatawakazia fikira kondoo wanaofutiliwa mbali.[i] Hatawatafuta wachanga, wala hatawaponya kondoo waliovunjika.[j] Anayesimama hatampa chakula, naye atakula nyama ya aliye mnono,[k] atazing’oa kwato za kondoo.[l] **17** Ole wake mchungaji wangu asiyefaa kitu,[m] anayeliacha kundi![n] Upanga utakuwa juu ya mkono wake na juu ya jicho lake la kuume. Mkono wake utakauka[o] bila shaka, na jicho lake la kuume bila shaka litaingia giza.”

12 Tangazo:
“Neno la Yehova kuhusu Israeli,” asema Yehova, Yeye anayetandaza mbingu[p] na kuweka msingi wa dunia[q] na kufanyiza roho[r] ya mwanadamu ndani yake. **2** “Tazama, mimi ninafanya Yerusalemu[s] kuwa bakuli linalosababisha kuyumba-yumba kwa

SURA 11

a Eze 8:18
b Eze 38:21 Mik 7:2 Hag 2:22 Zek 11:9 Zek 14:13
c Mt 22:7
d Zb 50:22 Ebr 10:27
e Zb 23:1 Zb 80:1 Zb 95:7 Isa 40:11
f Zek 11:4 Zek 13:8
g Sef 3:12 Zek 11:11
h 1Sa 17:40 Zb 23:4
i Zb 133:1 Zek 11:10
j Eze 37:19 Zek 11:14
k Ho 5:7
l Kum 32:19
m Yer 23:33 Zek 10:2
n Yer 15:2
o Yer 19:9 Eze 5:10
p Zb 90:17 Zek 11:7
q Mt 23:38
r Yer 14:21 Eze 16:59
s Isa 14:32 Sef 3:12
t Isa 8:17 Lu 2:25
u 1Fa 21:2
v Mt 26:15 Mt 27:9

Safu ya 2

a Mt 27:5
b Kut 21:32 Mk 14:11
c Mt 27:6 Mdo 1:18
d Zek 11:7
e Isa 11:13 Eze 37:16
f 1Fa 12:20 Isa 9:21
g Eze 34:2 Mt 15:14
h 1Pe 5:3
i Yer 23:2 Eze 34:6 Mt 9:36
j Eze 34:21
k Mwa 31:38 Eze 34:3
l Eze 34:10
m Yer 23:1 Eze 13:2 Mt 23:13
n Yoh 10:12
o 1Fa 13:4 Eze 30:22

SURA 12

p Ayu 26:7 Zb 104:2 Isa 42:5 Isa 44:24
q Zb 102:25; Zb 136:6; Isa 45:18; Isa 48:13; r Ayu 34:14; Zb 146:4; Mhu 12:7; Mdo 17:25; s Ebr 12:22.

vikundi vyote vya watu kuzunguka pande zote;[a] na pia atakuja kuzingira Yuda, naam, Yerusalemu.[b] **3** Na itatukia katika siku hiyo[c] kwamba nitafanya Yerusalemu kuwa jiwe[d] lenye kulemea vikundi vyote vya watu. Wale wote wanaoliinua bila shaka watajitia mikwaruzo mikali; na mataifa yote ya dunia hakika yatakusanyika[e] kupigana naye. **4** Katika siku hiyo,"[f] asema Yehova, "nitamtia mshangao kila farasi[g] na kumtia wazimu[h] mpandaji wake; nami nitafungua macho[i] yangu juu ya nyumba ya Yuda, nami nitampofusha kila farasi wa vikundi vya watu. **5** Na mashehe[j] wa Yuda watasema moyoni mwao, 'Wakaaji wa Yerusalemu ni nguvu kwangu katika Yehova wa majeshi Mungu wao.'[k] **6** Katika siku hiyo nitawafanya mashehe wa Yuda kama chombo cha moto kati ya miti[l] na kama mwenge wenye moto katika fungu la nafaka iliyokatwa hivi karibuni,[m] nao watateketeza vikundi vyote vya watu kuzunguka pande zote upande wa mkono wa kuume na wa kushoto;[n] na Yerusalemu litakaliwa tena na watu mahali pake mwenyewe, katika Yerusalemu.[o]

7 "Naye Yehova hakika ataokoa mahema ya Yuda kwanza, kusudi uzuri wa nyumba ya Daudi na uzuri wa wakaaji wa Yerusalemu usiwe mkuu mno kuliko Yuda. **8** Katika siku hiyo Yehova atakuwa ulinzi kuzunguka wakaaji wa Yerusalemu;[p] na yeye anayejikwaa kati yao atakuwa katika siku hiyo kama Daudi,[a] na nyumba ya Daudi kama Mungu,[b] kama malaika wa Yehova mbele yao.[c] **9** Na itatukia katika siku hiyo kwamba nitatafuta kuyaangamiza mataifa yote yanayokuja kupigana na Yerusalemu.[d]

10 "Nami nitamimina juu ya nyumba ya Daudi na juu ya wakaaji wa Yerusalemu roho ya kibali[e] na maombi,[f] nao watamtazama Yule waliyemchoma,[g] nao wataomboleza juu Yake kama kuombolezea mwana wa pekee; na kutakuwa na maombolezo machungu juu yake kama vile kunapokuwa na maombolezo juu ya mwana mzaliwa wa kwanza.[h] **11** Katika siku hiyo maombolezo katika Yerusalemu yatakuwa makubwa, kama maombolezo ya Hadadrimoni katika nchi tambarare ya bonde la Megido.[i] **12** Na nchi hakika itaomboleza,[j] kila familia peke yake; familia ya nyumba ya Daudi peke yake, na wanawake wao peke yao;[k] familia ya nyumba ya Nathani[l] peke yake, na wanawake wao peke yao; **13** familia ya nyumba ya Lawi[m] peke yake, na wanawake wao peke yao; familia ya Washimei[n] peke yake, na wanawake wao peke yao; **14** familia zote zitakazobaki, kila familia peke yake, na wanawake wao peke yao.[o]

13 "Katika siku hiyo[p] nyumba ya Daudi na wakaaji wa Yerusalemu watafunguliwa kisima[q] kwa ajili ya dhambi[r] na kwa ajili ya chukizo.[s]

SURA 12

a Zb 75:8
Zek 14:13
b Zek 14:14
c Sef 3:19
d Da 2:34
Da 2:45
Mt 21:44
e Zb 2:2
Eze 38:9
Mik 4:11
Zek 14:2
Ufu 16:14
f Isa 24:21
g Met 21:31
h Kum 28:28
Zb 76:6
i 1Fa 8:29
2Nya 7:15
Isa 37:17
j Zek 9:7
k Zb 46:1
Isa 41:10
Yoe 3:16
Zek 12:8
l Isa 10:17
Oba 18
m Isa 41:15
Isa 62:1
n Mik 4:13
Zek 9:15
o Yer 31:38
Zek 2:4
Zek 12:10
p Yer 23:6
Yoe 3:16
Zek 2:5
Zek 9:15

Safu ya 2

a Eze 34:24
b Zb 45:6
Isa 9:6
Ho 3:5
c Kut 14:19
Kut 23:20
d Isa 54:17
Hag 2:22
Ufu 16:14
e Isa 32:15
Isa 44:3
Yoe 2:28
Mdo 3:19
f 2Nya 6:21
Zb 28:2
Yer 31:9
g Yoh 19:34
Yoh 19:37
Yoh 20:27
Ufu 1:7
h Yer 6:26
Amo 8:10
i 2Fa 23:29
2Nya 35:22
j Yer 3:21
Lu 23:48
k Mk 15:40
Lu 23:49
l 2Sa 5:14
Lu 3:31
m Kut 6:16
n Kut 6:17
1Fa 1:8
1Nya 23:10
o Mk 15:41

SURA 13

p Zek 12:3
q Zb 51:7
r Isa 1:6; Eze 36:25; Yoh 1:29; Mdo 2:38; Mdo 2:41;
s 2Nya 29:5; Omb 1:8; Eze 36:17; Eze 36:29.

2 “Na itatukia katika siku hiyo,” asema Yehova wa majeshi, “kwamba nitakatilia mbali majina ya sanamu kutoka katika nchi,[a] nayo hayatakumbukwa tena kamwe; nami nitaondoa pia katika nchi manabii[b] na roho ya uchafu.[c] **3** Na itatukia kwamba mtu akitoa unabii tena, baba yake na mama yake, waliomzaa, watamwambia pia, ‘Wewe hutaishi, kwa maana umesema uwongo katika jina la Yehova.’ Na baba yake na mama yake, waliomzaa, watamchoma kwa silaha kwa sababu ametoa unabii.[d]

4 “Na itatukia katika siku hiyo kwamba manabii wataona aibu,[e] kila mmoja kwa sababu ya maono yake anapotoa unabii; nao hawatavaa vazi rasmi la manyoya[f] kwa kusudi la kudanganya. **5** Naye atasema, ‘Mimi si nabii. Mimi ni mtu anayelima udongo, kwa sababu mtu fulani wa udongo alinichukua tangu ujana wangu.’ **6** Na mtu atamwambia, ‘Haya majeraha mwilini mwako kati ya mikono yako ni nini?’ Naye atajibu, ‘Ni yale niliyotiwa nyumbani mwa wale wanaonipenda sana.’”

7 “Ee upanga, amka juu ya mchungaji[g] wangu, juu ya mwanamume ambaye ni mwenzangu,”[h] asema Yehova wa majeshi. “Mpige mchungaji,[i] na wale wa kundi watawanyike;[j] nami nitageuza mkono wangu juu ya wale wasio na maana.”[k]

8 “Na itatukia katika nchi yote,” asema Yehova, “kwamba sehemu mbili ndani yake ndizo zitakazokatiliwa mbali na kwisha;[a] lakini sehemu ya tatu itaachwa ndani yake.[b] **9** Nami nitaleta sehemu hiyo ya tatu kupitia moto;[c] nami nitawasafisha kama vile fedha inavyosafishwa,[d] na kuwajaribu kama vile dhahabu inavyojaribiwa.[e] Nayo italiitia jina langu, nami nitaijibu.[f] Nitasema, ‘Ni watu wangu,’[g] nayo itasema, ‘Yehova ni Mungu wangu.’”[h]

14 “Tazama! Kuna siku ambayo inakuja, siku ya Yehova,[i] na nyara yenu itagawanywa katikati yenu. **2** Nami nitakusanya mataifa yote yalete vita[j] juu ya Yerusalemu; na jiji hilo litatekwa[k] na nyumba zitanyakuliwa, na wanawake watalalwa kingu-vu.[l] Na nusu ya jiji itaenda uhamishoni;[m] lakini watu watakaobaki,[n] hawatakatiliwa mbali kutoka katika jiji hilo.[o]

3 “Na Yehova ataenda na kupiga vita juu ya mataifa[p] hayo kama katika siku yake ya vita, katika siku ya pigano.[q] **4** Na miguu yake itasimama katika siku hiyo juu ya mlima wa mizeituni, ulioko mbele ya Yerusalemu, upande wa mashariki;[r] na mlima wa mizeituni[s] utapasuliwa katikati,[t] kutoka mashariki na upande wa magharibi. Kutakuwa na bonde kubwa sana; na nusu ya mlima ule itasogezwa upande wa kaskazini, na nusu yake upande wa kusini. **5** Nanyi mtakimbilia bonde la milima yangu;[u] kwa sababu bonde la milima hiyo litafika mpaka Aseli. Nanyi mtakimbia, kama vile mlivyokimbia kwa sababu ya lile tetemeko la

SURA 13

a Kut 23:13
Kum 12:3
Isa 2:18
Eze 36:25
Sef 1:4
b Kum 13:5
Yer 8:10
Yer 23:14
Eze 14:9
c 2Ko 7:1
d Kum 13:6
Kum 13:9
Kum 18:20
Mt 10:37
e Yer 2:26
Mik 3:7
f 2Fa 1:8
Mt 3:4
g Eze 34:23
Mik 5:4
Mt 26:55
Yoh 10:11
Ebr 13:20
1Pe 5:4
h Met 8:30
Yoh 1:1
Yoh 16:28
Yoh 17:5
i Isa 53:8
Da 9:26
Mk 14:27
Mdo 3:18
Ufu 13:8
j Mt 26:31
Mk 14:50
Yoh 16:32
k Isa 1:25
Mt 11:25
1Ko 1:27

Safu ya 2

a Mt 13:41
Lu 12:46
b Yoe 2:32
Mt 24:22
Ro 9:27
c Isa 43:2
d Zb 66:10
Isa 48:10
Mal 3:2
e Mal 3:3
1Pe 1:7
f Isa 58:9
g Yer 30:22
Ro 9:25
h Zb 144:15
Ufu 21:7

SURA 14

i Isa 2:12
Yoe 2:31
2Pe 3:10
j Yoe 3:2
Ufu 16:14
k Lu 21:20
l Kum 28:30
Omb 5:11
m Lu 21:24
n Isa 65:8
Mt 21:43
Mt 24:22
o Isa 65:18
Ebr 12:22
Ufu 21:2
p Isa 66:16
Eze 38:23
Yoe 3:14
Ufu 16:14
q Kut 15:3
2Nya 20:15
r Eze 11:23
Mdo 1:12
s Lu 19:29
t Mik 1:4
u Lu 21:21

nchi katika siku za Uzia mfalme wa Yuda.[a] Na Yehova Mungu wangu atakuja,[b] watakatifu wote wakiwa pamoja naye.[c]

6 "Na itatukia katika siku hiyo kwamba nuru[d] yenye thamani haitakuwapo—vitu vitagandamana.[e] **7** Nayo itakuwa siku moja inayojulikana kuwa ni ya Yehova.[f] Haitakuwa mchana, wala haitakuwa usiku;[g] na itatukia kwamba wakati wa jioni kutakuwa na nuru.[h] **8** Na itatukia siku hiyo kwamba maji yaliyo hai[i] yatatoka katika Yerusalemu,[j] nusu yake kuelekea upande wa bahari ya mashariki[k] na nusu yake kuelekea upande wa bahari ya magharibi.[l] Itakuwa hivi wakati wa kiangazi na wa majira ya baridi kali.[m] **9** Na Yehova atakuwa mfalme juu ya dunia yote.[n] Katika siku hiyo Yehova atakuwa mmoja,[o] na jina lake litakuwa moja.[p]

10 "Nchi yote itageuzwa na kuwa kama Araba,[q] kutoka Geba[r] mpaka Rimoni[s] upande wa kusini wa Yerusalemu; nalo litainuka na kukaliwa na watu mahali pake,[t] kutoka Lango la Benyamini[u] mpaka mahali pa Lango la Kwanza, mpaka Lango la Pembeni, na kutoka Mnara wa Hananeli[v] mpaka mitungi ya kushinikizia ya mfalme. **11** Na watu watakaa ndani yake; wala kutengwa kwa ajili ya maangamizi hakutatokea tena,[w] na Yerusalemu litakaliwa katika usalama.[x]

12 "Na hii ndiyo tauni ambayo Yehova atatumia kuwapiga watu wote watakaofanya mapigano ya kijeshi juu ya Yerusalemu:[a] Nyama ya mtu itaoza, huku akiwa amesimama kwa miguu yake;[b] na macho ya mtu yataoza yakiwa katika matundu yake, na ulimi wake utaoza ukiwa kinywani mwake.

13 "Na itatukia katika siku hiyo kwamba mvurugo kutoka kwa Yehova utaenea katikati yao;[c] na kila mmoja wao ataukamata mkono wa mwenzake, na mkono wake utainuka juu ya mkono wa mwenzake. **14** Yuda nayo pia itapiga vita katika Yerusalemu; na mali za mataifa yote kuzunguka pande zote zitakusanywa, dhahabu na fedha na mavazi kwa wingi mno.[d]

15 "Na hivyo ndivyo tauni ya farasi, nyumbu, ngamia, na punda-dume, na kila aina ya mnyama wa kufugwa atakayekuwa katika kambi hizo, itakavyokuwa, kama tauni hiyo.

16 "Na itatukia kwamba, kila mtu atakayebaki wa mataifa yote yanayokuja juu ya Yerusalemu,[e] watapanda pia mwaka baada ya mwaka[f] ili kumwinamia Mfalme,[g] Yehova wa majeshi,[h] na kufanya sherehe ya vibanda.[i] **17** Na itatukia kwamba, yeyote asiyepanda[j] kuja Yerusalemu kutoka katika familia[k] za dunia ili kumwinamia Mfalme, Yehova wa majeshi, mvua haitamnyeshea.[l] **18** Na watu wa familia ya Misri wasipokuja wala kuingia, mvua pia haitakuwa juu yao. Kutatokea tauni ambayo Yehova hutumia kuyapiga yale mataifa yasiyopanda kuja kufanya sherehe ya vibanda. **19** Hiyo ndiyo itakayokuwa adhabu kwa ajili ya dhambi

SURA 14

a Amo 1:1
b Zb 96:13
Zb 98:9
Yud 14
c Kum 33:2
Zb 149:9
Yoe 3:11
d Isa 13:10
Amo 5:18
e Kut 15:8
Ayu 38:22
f Zb 118:24
1Th 5:2
2Th 2:2
g Zb 97:11
Met 4:18
Ufu 21:25
h Isa 30:26
i Yoh 4:10
Ufu 21:6
Ufu 22:17
j Yer 17:13
Eze 47:1
Yoe 3:18
Ufu 22:1
k Kum 3:17
Eze 47:8
l Yos 1:4
Yoe 2:20
m Isa 49:10
n Zb 97:1
Ufu 19:6
o Kum 6:4
Mal 2:10
Ga 3:20
p Isa 42:8
Isa 44:6
q Kum 1:7
r 1Fa 15:22
s 1Nya 4:32
t Yer 30:18
u Yer 37:13
Eze 48:32
v Ne 3:1
Yer 31:38
w Isa 60:18
Yer 31:40
x Yer 23:6
Yer 33:16

Safu ya 2

a 2Fa 19:35
Zb 110:5
Yoe 3:2
Mik 4:11
Ufu 16:14
b Mdo 12:23
c Amu 7:22
Eze 38:21
Zek 11:6
d 2Nya 14:13
2Nya 20:25
Zek 2:9
e Isa 66:19
Mdo 15:17
f 1Sa 1:7
Isa 66:23
g Zb 86:9
Isa 27:13
Yer 48:15
Ro 15:11
h Zb 24:8
Zb 103:21
i Law 23:34
Ne 8:14
Yoh 7:2
j Isa 45:23
Isa 60:12
k Mwa 10:32
Yer 10:25
Amo 3:2
l Kum 11:17
1Fa 8:35
Isa 5:6

ya Misri na dhambi ya mataifa yote yasiyopanda kuja kufanya sherehe ya vibanda.[a]

20 "Katika siku hiyo juu ya kengele za farasi kutakuwa na[b] maneno 'Utakatifu ni wa Yehova!'[c] Na vyungu vya kupikia vyenye mdomo mpana[d] vilivyo katika nyumba ya Yehova vitakuwa kama mabakuli[e] yaliyo mbele ya madhabahu.[f] **21** Na kila chungu cha kupikia chenye mdomo mpana katika Yerusalemu na katika Yuda kitakuwa kitu kitakatifu kwa Yehova wa majeshi, na wale wote wanaotoa dhabihu wataingia na kuchukua kutoka ndani yake na kuchemshia ndani yake.[a] Na katika siku hiyo hakutakuwa na Mkanaani[b] tena katika nyumba ya Yehova wa majeshi."[c]

SURA 14
a Kol 2:17; Ebr 10:1
b Mal 1:11
c Kut 28:36; Kut 39:30; Isa 35:8
d 1Sa 2:14
e Kut 25:29; Kut 37:16; Hes 4:7
f 2Nya 29:22

Safu ya 2
a Kum 16:7; 1Sa 2:13; Eze 46:23

b Isa 35:8; Eze 44:9; Ufu 21:27; c 1Ti 3:15.

MALAKI

1 Tangazo:
Neno la Yehova[a] kuhusu Israeli kupitia Malaki:

2 "Nimewapenda ninyi,"[b] Yehova amesema.

Nanyi mmesema: "Umetupenda kwa njia gani?"[c]

"Je, Esau hakuwa ndugu ya Yakobo?"[d] asema Yehova. "Lakini nilimpenda Yakobo,[e] **3** naye Esau[f] nikamchukia; mwishowe nikafanya milima yake kuwa ukiwa[g] na urithi wake kuwa wa mbwa-mwitu wa nyikani."[h]

4 "Kwa sababu Edomu anaendelea kusema, 'Tumevunjwa-vunjwa, lakini tutarudi na kujenga mahali palipoharibiwa,' Yehova wa majeshi amesema hivi, 'Wao watajenga; lakini mimi nitabomoa.[i] Na watu watawaita wao kuwa "eneo la uovu" na "watu ambao Yehova ameshutumu[j] mpaka wakati usio na kipimo." **5** Na macho yenu wenyewe yataona hilo, nanyi mtasema: "Yehova na atukuzwe juu ya eneo la Israeli."'"[a]

6 "'Mwana humheshimu baba;[b] na mtumishi humheshimu bwana-mkuu wake.[c] Basi ikiwa mimi ni baba,[d] iko wapi heshima yangu?[e] Na ikiwa mimi ni Bwana-Mkuu, uko wapi woga[f] kwa ajili yangu?' Yehova wa majeshi amewaambia ninyi, enyi makuhani mnaolidharau jina langu.[g]

"'Nanyi mmesema: "Tumelidharau jina lako kwa njia gani?"'

7 "'Kwa kutoa juu ya madhabahu yangu mkate uliotiwa unajisi.'[h]

"'Nanyi mmesema: "Tumekutia unajisi kwa njia gani?"'

"'Kwa kusema: "Meza[i] ya Yehova ni kitu cha kudharauliwa."[j] **8** Na mnapotoa mnyama kipofu kwa ajili ya dhabihu mnasema: "Si vibaya." Na mnapotoa mnyama kilema au mgonjwa mnasema: "Si vibaya."'"[k]

SURA 1
a 2Pe 1:21
b Kum 7:6; Kum 10:15; Isa 41:8; Ro 11:28
c Isa 49:14
d Mwa 25:25
e Ro 9:13
f Mwa 25:34; Mwa 27:41; Ebr 12:16
g Isa 34:10; Yer 49:20; Eze 25:13; Eze 35:3; Yoe 3:19; Oba 10
h Isa 34:13
i Ayu 12:14; Zb 127:1
j Zb 137:7; Isa 34:5; Oba 18

Safu ya 2
a Zb 35:27
b Kut 20:12; Mt 15:4; Mk 10:19; Efe 6:2
c 1Ti 6:1; Tit 2:9
d Kut 4:22
e Isa 1:2; Mt 6:9
f Met 8:13; 1Pe 2:17
g Yer 5:31; Yer 23:11; Eze 22:26; Ho 4:6
h Law 21:6
i Eze 41:22; 1Ko 10:21
j 1Sa 2:17
k Law 22:20; Kum 15:21

"Tafadhali, mleteni kwa gavana wenu. Je, atawafurahia ninyi, au je, atawapokea kwa fadhili?" Yehova wa majeshi amesema.

9 "Na sasa, tafadhali, utulizeni uso[a] wa Mungu, ili apate kutuonyesha kibali.[b] Jambo hilo limetoka mkononi mwenu. Je, atampokea yeyote wenu kwa fadhili?" Yehova wa majeshi amesema.

10 "Ni nani pia aliye kati yenu atakayefunga milango?[c] Nanyi hamtaiwasha madhabahu yangu—bure.[d] Sipendezwi nanyi hata kidogo," Yehova wa majeshi amesema, "nami sifurahii toleo la zawadi kutoka mkononi mwenu."[e]

11 "Kwa maana tangu kuchomoza kwa jua mpaka kutua kwake jina langu litakuwa kuu kati ya mataifa,[f] na kila mahali moshi wa dhabihu[g] utafukizwa, toleo litafanywa kwa jina langu, pia zawadi safi;[h] kwa kuwa jina langu litakuwa kuu kati ya mataifa,"[i] Yehova wa majeshi amesema.

12 "Lakini ninyi mnanitia unajisi[j] kwa kusema, 'Meza ya Yehova ni kitu kilichotiwa unajisi, na matunda ya meza hiyo, yaani, chakula cha meza hiyo, ni kitu cha kudharauliwa.'[k] **13** Nanyi mmesema, 'Tazama! Jambo hili linachosha kama nini!'[l] nanyi mmeitolea pumzi puani kwa dharau," Yehova wa majeshi amesema. "Nanyi mmeleta kitu ambacho kimenyakuliwa, na chenye kilema, na kilicho kigonjwa;[m] ndiyo, mmekileta kama zawadi. Je, naweza kukifurahia mkononi mwenu?"[n] Yehova amesema.

SURA 1

a Kut 32:11
Yer 26:19
Yoe 1:13
Yoe 1:14
b Yoe 2:17
c 2Nya 23:4
d Yer 6:13
Mik 3:11
e Isa 1:11
Yer 6:20
Yer 14:12
Amo 5:21
f Zb 113:3
Isa 45:6
Isa 59:19
Zek 14:16
g Zb 66:15
Ro 12:1
Ebr 13:15
h Isa 66:20
Yoh 4:23
i Zb 22:27
Sef 3:9
Mt 28:19
Ufu 15:4
j Eze 22:26
k Mal 1:7
l Isa 43:22
Mik 6:3
m Kum 15:21
Kum 17:1
n Law 22:20
Isa 1:13
Mal 2:13

Safu ya 2

a Mdo 5:3
b Zb 47:2
Yer 10:10
Da 9:4
c Zb 76:12
Ufu 15:4

SURA 2

d Omb 4:13
Ho 5:1
Mal 1:6
e Law 26:14
Isa 30:9
f Zb 81:11
Isa 42:25
Isa 57:11
g Yer 13:16
h Kum 28:15
i Ho 4:7
Hag 1:11
j Ho 8:7
Yoe 1:17
k Yer 28:9
Eze 33:33
l Kut 40:15
m Hes 3:6
Hes 18:23
Eze 44:15
n Zb 119:165
o Zb 19:9
Zb 111:10
p Zb 111:9
q 2Nya 17:9
Eze 44:24
r Kut 32:26
s Yak 5:20

14 "Naye amelaaniwa anayetenda kwa ujanja wakati kuna mnyama dume katika kundi lake, naye anaweka nadhiri na kutoa dhabihu ya kilema kwa Yehova.[a] Kwa maana mimi ni Mfalme mkuu,"[b] Yehova wa majeshi amesema, "na jina langu litakuwa lenye kuogopesha kati ya mataifa."[c]

2 "Na sasa amri hii inawahusu ninyi, enyi makuhani.[d] **2** Ikiwa hamtasikiliza,[e] na ikiwa hamtaiweka moyoni[f] ili kulipa jina langu utukufu,"[g] Yehova wa majeshi amesema, "mimi pia nitaleta juu yenu laana,[h] nami nitazilaani baraka zenu.[i] Ndiyo, hata nimeilaani baraka, kwa sababu hamwitii moyoni."

3 "Tazama! Naikemea mbegu iliyopandwa kwa sababu yenu,[j] nami nitawapaka mavi juu ya nyuso zenu, mavi ya sherehe zenu; na mtu fulani atawapeleka mahali ilipo. **4** Nanyi mtajua kwamba nimewapelekea ninyi amri hii,[k] ili agano[l] langu pamoja na Lawi liendelee,"[m] Yehova wa majeshi amesema.

5 "Nalo agano langu lilikuwa naye, ambalo ni la uzima na la amani,[n] nami nikaendelea kumpa hayo, pamoja na woga. Naye akaendelea kuniogopa;[o] ndiyo, kwa sababu ya jina langu yeye mwenyewe aliingiwa na hofu.[p] **6** Sheria ya kweli ilikuwa katika kinywa chake,[q] wala ukosefu wa uadilifu haukupatikana midomoni mwake. Kwa amani na kwa unyoofu alitembea nami,[r] na wale aliogeuza kutoka katika kosa walikuwa wengi.[s] **7** Kwa maa-

na midomo ya kuhani ndiyo
inayopaswa kutunza ujuzi, na
sheria ndiyo ambayo watu wa-
napaswa kutafuta kutoka ki-
nywani mwake;[a] kwa maana
yeye ndiye mjumbe wa Yehova
wa majeshi.[b]
8 "Lakini ninyi—mmegeuka
kando mkaiacha njia.[c] Mmesa-
babisha wengi kujikwaa kati-
ka sheria.[d] Mmeliharibu agano
la Lawi,"[e] Yehova wa majeshi
amesema. **9** "Nami pia, kwa
upande wangu, nitawafanya
mdharauliwe na kuwa wa hali
ya chini kwa watu wote,[f] kama
vile ambavyo ninyi hamkuwa
mkizishika njia zangu, lakini
mlikuwa mkionyesha ubaguzi
katika sheria."[g]
10 "Je, sisi sote hatuna
baba mmoja?[h] Je, sisi hatu-
kuumbwa na Mungu mmoja?[i]
Kwa nini basi tunatendeana
kwa hila,[j] katika kutia una-
jisi agano la mababu zetu?[k]
11 Yuda ametenda kwa hila,
na chukizo limefanywa kati-
ka Israeli na katika Yerusale-
mu;[l] kwa maana Yuda ameu-
tia unajisi utakatifu wa Yeho-
va,[m] ambao Yeye amependa,
naye amemchukua binti ya
mungu wa kigeni awe bibi-aru-
si.[n] **12** Yehova atamkatilia
mbali kila mmoja anayefanya
hivyo,[o] yeye ambaye yuko ma-
cho na yeye anayejibu, kuto-
ka katika mahema ya Yakobo,
na yeye anayemtolea Yehova
wa majeshi toleo la zawadi."[p]
13 "Hili nalo ndilo jambo la
pili ambalo ninyi hufanya,
na matokeo yake ni madha-
bahu ya Yehova kufunikwa
kwa machozi, kwa kulia na
kuugua, hivi kwamba haku-

SURA 2
a Law 10:11
Kum 24:8
2Nya 15:3
Ne 8:8
b Hag 1:13
c Isa 1:4
Isa 30:9
Ebr 3:12
d Yer 18:15
Lu 11:52
e Ne 13:29
f 1Sa 2:30
Mik 3:7
g Law 19:15
Kum 1:17
Kum 16:19
Yak 2:9
h 1Ko 8:6
Efe 4:6
i Mwa 2:7
Zb 100:3
Mdo 17:25
j Ne 5:8
Mik 7:2
k Yos 23:16
l Yer 7:10
m Law 20:26
n Kum 7:3
Amu 3:6
1Fa 11:1
Ne 13:23
o Hes 15:31
p 1Sa 15:22
Amo 5:22

Safu ya 2
a Met 21:27
Isa 1:11
b Yer 8:12
c Met 5:18
Mhu 9:9
d Met 2:17
Mt 19:5
e Mwa 3:15
Mdo 3:25
Ga 3:16
f Met 25:28
g Kum 22:13
h Mwa 2:24
Mt 5:32
Mt 19:8
Mk 10:9
i Zb 11:5
Isa 59:6
j Yer 5:11
Ho 5:7
Mal 2:10
k Isa 1:15
Isa 7:13
Isa 43:24
Yer 15:6
l Met 30:12
Eze 18:29
m Kum 32:4
Zb 37:28
Isa 58:2

SURA 3
n Mt 11:10
Lu 1:76
Yoh 1:6
o Mt 3:3
Mk 1:3
Yoh 1:23
Yoh 3:28
Mdo 13:24
Mdo 19:4

na tena kugeukia toleo la za-
wadi wala kufurahia kitu cho-
chote kutoka mkononi mwe-
nu.[a] **14** Nanyi mmesema,
'Kwa sababu gani?'[b] Kwa sa-
babu hii, kwamba Yehova ame-
toa ushahidi kati yako na mke
wa ujana wako,[c] ambaye wewe
umemtendea kwa hila, inga-
wa yeye ni mwenzako naye ni
mke wa agano lako.[d] **15** Na
kuna mtu ambaye hakufanya
hivyo, kwa vile alikuwa na
baki la roho. Huyo naye ali-
kuwa akitafuta nini? Uzao wa
Mungu.[e] Nanyi jilindeni kuhu-
siana na roho yenu,[f] na yeyote
asimtendee kwa hila mke wa
ujana wake.[g] **16** Kwa maana
yeye amechukia talaka,"[h] Ye-
hova, Mungu wa Israeli, ame-
sema; "na yule ambaye ame-
funika vazi lake kwa jeuri,"[i]
Yehova wa majeshi amesema.
"Nanyi mjilinde roho yenu, na-
nyi msitende kwa hila.[j]
17 "Ninyi mmemchosha Ye-
hova kwa maneno yenu,[k] na-
nyi mmesema, 'Tumemchosha
kwa njia gani?' Kwa kusema,
'Kila mtu anayefanya mabaya
ni mwema machoni pa Yehova,
naye amependezwa na watu
wa aina hiyo';[l] au, 'Yuko wapi
Mungu wa haki?' "[m]
3 "Tazama! ninamtuma mju-
mbe wangu,[n] naye atafu-
ngua njia mbele zangu.[o] Na
kwa ghafula Bwana wa kweli[p]
atakuja kwenye hekalu Lake,[q]
ambaye ninyi mnamtafuta, na
mjumbe[r] wa agano[s] mnayepe-
ndezwa naye.[t] Tazama! Ata-
kuja hakika," asema Yehova
wa majeshi.[u]

p Zb 11:4; Isa 6:1; Ufu 11:19; q Mt 21:12; r Isa 63:9; Mt 15:24; Lu 1:69; s Kut 2:24; Lu 1:72; t Yoh 12:19; u Isa 44:26.

2 "Lakini ni nani atakayeistahimili siku ya kuja kwake,[a]
naye ni nani atakayesimama
wakati atakapoonekana?[b] Kwa
maana atakuwa kama moto wa
msafishaji[c] na kama sabuni[d]
ya wafuaji wa nguo.[e] **3** Naye
ataketi kama msafishaji na
mtakasaji wa fedha[f] naye ata-
watakasa wana wa Lawi;[g] naye
atawasafisha kama dhahabu[h]
na kama fedha, nao watakuwa
kwa Yehova watu wanaotoa toleo la zawadi[i] katika uadilifu. **4** Na toleo la zawadi
la Yuda na la Yerusalemu litakuwa lenye kumpendeza Yehova,[j] kama katika siku za zamani na kama katika miaka ya kale.[k]

5 "Nami nitawakaribia ninyi ili kuhukumu,[l] nami nitakuwa shahidi wa haraka[m] juu
ya walozi,[n] na juu ya wazinzi,[o]
na juu ya wale wanaoapa kwa
uwongo,[p] na juu ya wale wanaoupunja mshahara wa mfanyakazi,[q] na mjane[r] na mvulana asiye na baba,[s] na wale
wanaomfukuza mkaaji mgeni,[t]
wala hawakuniogopa mimi,"[u]
Yehova wa majeshi amesema.

6 "Kwa maana mimi ni Yehova; sikubadilika.[v] Nanyi
ni wana wa Yakobo; hamjafikia mwisho wenu.[w] **7** Tangu
siku za mababu zenu mmeyaacha masharti yangu wala hamkuyashika.[x] Rudini kwangu,
nami nitarudi kwenu,"[y] Yehova wa majeshi amesema.

Nanyi mmesema: "Tutarudi
kwa njia gani?"

8 "Je, mtu wa udongo atamnyang'anya Mungu? Lakini ninyi mnaninyang'anya
mimi."

SURA 3

a Amo 5:18
b Mt 24:13
Lu 21:36
c Da 11:35
Da 12:10
1Ko 3:13
d Yer 2:22
e Isa 1:25
f Zb 66:10
Met 25:4
Zek 13:9
g Yer 33:18
Ufu 1:6
h 1Pe 1:7
i Zb 69:31
Ebr 13:15
1Pe 2:5
j Mal 1:11
k 2Nya 7:1
Yer 2:2
l Ebr 10:30
m Mik 1:2
Ufu 22:12
n Ufu 21:8
o Yer 29:23
p Kut 20:7
q Zb 62:10
Met 14:31
Yak 5:4
r Kum 24:17
Lu 20:47
s Isa 1:17
Yak 1:27
t Kut 23:9
Zek 7:10
u Met 8:13
v Isa 43:10
Isa 46:4
Yak 1:17
w Zb 105:8
Omb 3:22
Ro 11:29
x Kum 9:7
Ne 9:26
Mdo 7:51
y Kum 4:30
Yer 3:12
Zek 1:3
Yak 4:8

Safu ya 2

a Law 24:15
Isa 8:21
b Law 27:30
Kum 14:28
c 2Nya 31:11
Ne 12:44
Ne 13:10
d 2Ko 9:8
e Kum 28:12
2Fa 7:19
f Law 26:10
2Nya 31:10
Met 3:10
Met 10:22
g Yoe 1:4
Amo 4:9
Amo 7:1
h Kum 11:14
Yoe 2:24
Zek 8:12

Nanyi mmesema: "Tumekunyang'anya kwa njia gani?"

"Katika sehemu za kumi na
katika michango. **9** Kwa laana mnanilaani,[a] nanyi mnaninyang'anya mimi—taifa zima.
10 Leteni ghalani sehemu
zote za kumi,[b] ili kuwe na chakula nyumbani mwangu;[c] nanyi, tafadhali, mnijaribu kwa
njia hii,"[d] Yehova wa majeshi
amesema, "kama sitawafungulia ninyi malango ya mbinguni[e]
na kuwamwagia baraka hata
kusiwe na uhitaji tena."[f]

11 "Nami kwa ajili yenu nitakikemea kile kinachokula,[g]
nacho hakitawaharibia mazao
ya udongo, wala mzabibu ulio
shambani hautakuwa bila matunda kwenu,"[h] Yehova wa majeshi amesema.

12 "Na mataifa yote yatawatangaza ninyi kuwa wenye furaha,[i] kwa maana ninyi wenyewe mtakuwa nchi yenye kupendeza,"[j] Yehova wa majeshi
amesema.

13 "Maneno yenu yamekuwa yenye nguvu kinyume
changu,"[k] Yehova amesema.

Nanyi mmesema: "Sisi tumesemezana nini kinyume
chako?"[l]

14 "Mmesema, 'Hakuna faida kumtumikia Mungu.[m] Na
kwa vile tumeshika wajibu
wetu kwake, na tumetembea
kwa huzuni kwa sababu ya
Yehova wa majeshi, kuna faida gani?[n] **15** Na sasa tuna-
watangaza watu wenye kimbelembele kuwa wenye furaha.[o]
Pia, watendaji wa uovu wame-

i Zb 72:17; Isa 61:9; j Isa 62:4; k Isa 5:19; Isa 28:14; l Ayu 40:8; Mal 1:6; m Ayu 21:15; Zb 73:13; Isa 58:3; Sef 1:12; n Zek 7:5; Yak 4:9; o Zb 10:3; Zb 49:18.

jengwa.[a] Wao pia wamemjaribu Mungu nao huendelea kuponyoka.'"[b]

16 Wakati huo wale wenye kumwogopa Yehova[c] wakasemezana, kila mmoja na mwenzake, na Yehova akaendelea kutoa uangalifu na kusikiliza.[d] Na kitabu cha kumbukumbu kikaanza kuandikwa mbele zake[e] kwa ajili ya wale wenye kumwogopa Yehova na kwa ajili ya wale wanaolifikiria jina lake.[f]

17 "Nao watakuwa wangu,"[g] Yehova wa majeshi amesema, "siku ile nitakapotokeza mali ya pekee.[h] Nami nitawaonyesha huruma, kama vile mwanamume anavyomwonyesha huruma mwana wake ambaye anamtumikia.[i] **18** Nanyi mtaona tena tofauti kati ya mwadilifu na mwovu,[j] kati ya mtu anayemtumikia Mungu na mtu ambaye hajamtumikia."[k]

4 "Kwa maana, tazama! siku ile inakuja ambayo inawaka kama tanuru,[l] na wote wenye kimbelembele na wote wanaotenda uovu watakuwa kama majani makavu.[m] Na siku hiyo inayokuja itawateketeza," Yehova wa majeshi amesema, "hivi kwamba haitawaachia wao mzizi wala tawi.[a] **2** Na kwenu ninyi mnaoliogopa jina langu, jua la uadilifu litaangaza,[b] likiwa na kiponyaji katika mabawa yake;[c] nanyi mtatoka nje na kuukanyaga udongo kama ndama waliononeshwa."[d]

3 "Nanyi mtawakanyagia chini waovu, kwa maana watakuwa kama mavumbi chini ya nyayo za miguu yenu siku ile nitakayochukua hatua,"[e] asema Yehova wa majeshi.

4 "Ikumbukeni sheria ya Musa mtumishi wangu niliyomwamuru katika Horebu kuhusu Israeli wote, hata masharti na maamuzi ya hukumu.[f]

5 "Tazama! Nawatumia ninyi nabii Eliya[g] kabla ya kuja kwa ile siku ya Yehova iliyo kuu na yenye kuogopesha.[h] **6** Naye atageuza moyo wa akina baba urudi kwa wana, na moyo wa wana urudi kwa akina baba; ili nisije kuipiga dunia na kuiangamiza."[i]

SURA 3

a Yer 12:1
b Mhu 8:11
c Mwa 22:12; Zb 66:16; Mdo 9:31; Ufu 15:4
d Mt 18:19
e Zb 56:8; Zb 69:28; Zb 139:16
f Zb 20:7; Isa 26:8
g Yer 31:33; Yoh 17:9
h Isa 62:3; 1Pe 2:9
i Zb 103:13
j Zb 58:11; Ro 2:6
k Da 12:3; Mt 13:43

SURA 4

l Zb 21:9; Sef 2:2; Mt 13:42; 2Th 1:8; 2Pe 3:7
m Kut 15:7; Isa 5:24; Oba 18; Mt 3:12

Safu ya 2

a Ho 9:16; Amo 2:9
b Isa 30:26; Lu 1:78; Efe 5:14
c Zb 147:3; Yer 30:17; Yer 33:6
d Isa 49:9
e Mwa 3:15; Mik 7:10; Zek 10:5; Ro 16:20
f Kum 4:5; Zb 119:4; Zb 147:19
g Isa 40:3; Mt 11:14; Mk 9:11; h Yoe 2:31; Mdo 2:20; 2Pe 3:10; i Kum 29:20; Zek 14:11; Lu 1:17.

(Mwisho wa tafsiri ya Maandiko ya Kiebrania na Kiaramu.
Tafsiri inayofuata ni ya Maandiko ya Kigiriki ya Kikristo)

KULINGANA NA

MATHAYO

1 Kitabu cha historia[a] ya Yesu
Kristo, mwana wa Daudi,[b]
mwana wa Abrahamu:[c]
2 Abrahamu akamzaa
Isaka;[d]
Isaka akamzaa Yakobo;[e]
Yakobo akamzaa Yuda[f] na
ndugu zake;
3 Yuda akamzaa Perezi[g] na
Zera kwa Tamari;
Perezi akamzaa Hezroni;[h]
Hezroni akamzaa Ramu;[i]
4 Ramu akamzaa
Aminadabu;
Aminadabu akamzaa
Nashoni;[j]
Nashoni akamzaa
Salmoni;[k]
5 Salmoni akamzaa Boazi
kwa Rahabu;[l]
Boazi akamzaa Obedi kwa
Ruthu;[m]
Obedi akamzaa Yese;[n]
6 Yese akamzaa Daudi[o]
mfalme.[p]
Daudi akamzaa
Sulemani[q] kupitia mke
wa Uria;
7 Sulemani akamzaa
Rehoboamu;[r]
Rehoboamu akamzaa
Abiya;
Abiya[s] akamzaa Asa;[t]
8 Asa akamzaa
Yehoshafati;[u]
Yehoshafati akamzaa
Yehoramu;[v]
Yehoramu akamzaa Uzia;
9 Uzia akamzaa Yothamu;
Yothamu[w] akamzaa
Ahazi;[x]
Ahazi akamzaa Hezekia;[y]
10 Hezekia akamzaa
Manase;[z]

SURA 1

a Mwa 5:1
b 1Nya 17:11
Mt 9:27
Lu 1:32
c Mwa 22:18
d Mwa 21:3
1Nya 1:28
Lu 3:34
e Mwa 25:26
1Nya 1:34
f Mwa 29:35
g Mwa 38:29
1Nya 2:4
h Ru 4:18
Lu 3:33
i 1Nya 2:9
j Hes 2:3
Ru 4:20
1Nya 2:10
Lu 3:32
k 1Nya 2:11
l Yos 2:1
m Ru 4:13
n 1Nya 2:12
o Ru 4:17
1Nya 2:15
p 2Sa 5:4
q 2Sa 12:24
1Nya 3:5
Lu 3:31
r 1Fa 11:43
s 1Nya 3:10
t 2Nya 14:1
u 1Fa 15:24
v 1Nya 3:11
2Nya 21:1
w 2Fa 15:32
x 2Fa 15:38
y 2Fa 18:1
1Nya 3:13
z 2Fa 20:21

Safu ya 2

a 2Fa 21:18
b 2Nya 33:20
c 2Fa 21:24
1Nya 3:14
d 2Fa 23:34
e 1Nya 3:15
1Nya 3:16
Yer 28:4
f 2Fa 24:15
2Nya 36:10
Yer 27:20
Yer 29:2
g 1Nya 3:17
Lu 3:27
h 1Nya 3:19
Ezr 3:2
Ne 12:1
Lu 3:27
i Mt 13:55
Mk 6:3
j Mt 27:17
k Lu 1:27
l Lu 1:35

Manase[a] akamzaa Amoni;[b]
Amoni[c] akamzaa Yosia;
11 Yosia[d] akamzaa Yekonia[e]
na ndugu zake wakati
wa ule uhamisho wa
kwenda Babiloni.[f]
12 Baada ya ule uhamisho
wa kwenda Babiloni
Yekonia akamzaa
Shealtieli;[g]
Shealtieli akamzaa
Zerubabeli;[h]
13 Zerubabeli akamzaa
Abiudi;
Abiudi akamzaa Eliakimu;
Eliakimu akamzaa Azori;
14 Azori akamzaa Sadoki;
Sadoki akamzaa Akimu;
Akimu akamzaa Eliudi;
15 Eliudi akamzaa Eleazari;
Eleazari akamzaa Mathani;
Mathani akamzaa Yakobo;
16 Yakobo akamzaa Yosefu
mume wa Maria,
ambaye kwake Yesu
alizaliwa,[i] anayeitwa
Kristo.[j]

17 Basi, vizazi vyote kutoka Abrahamu mpaka Daudi vilikuwa vizazi kumi na vinne, na kutoka Daudi mpaka uhamisho wa kwenda Babiloni vizazi kumi na vinne, na kutoka uhamisho wa kwenda Babiloni mpaka Kristo vizazi kumi na vinne.

18 Lakini kuzaliwa kwa Yesu Kristo kulikuwa katika njia hii. Katika wakati ambapo Maria mama yake alikuwa amechumbiwa[k] na Yosefu, alionekana kuwa ana mimba kwa njia ya roho takatifu[l] ka-

bla ya wao kuungana pamoja.
19 Hata hivyo, Yosefu mume
wake, kwa sababu alikuwa
mwadilifu na hakutaka ku-
mtia aibu mbele ya watu,[a] ali-
kusudia kumtaliki[b] kwa siri.
20 Lakini alipokuwa amekwi-
sha kufikiria mambo haya, ta-
zama! malaika wa Yehova ali-
mtokea katika ndoto, akise-
ma: "Yosefu, mwana wa Dau-
di, usiogope kumchukua Maria
mke wako na kwenda naye
nyumbani, kwa maana mimba
iliyo ndani yake imetokana
na roho takatifu.[c] **21** Yeye
atazaa mwana, nawe lazima
umwite jina lake Yesu,[d] kwa
maana ataokoa[e] watu wake[f]
kutoka katika dhambi zao."[g]
22 Yote haya kwa kweli yalitu-
kia ili litimizwe lile lililosemwa
na Yehova[h] kupitia nabii wake,[i]
akisema: **23** "Tazama! Bikira[j]
atapata mimba naye atazaa
mwana, nao watamwita jina
lake Imanueli,"[k] ambalo lina-
potafsiriwa humaanisha, "Mu-
ngu Yuko Pamoja Nasi."[l]

24 Ndipo Yosefu akaamka
kutoka katika usingizi na ku-
fanya kama malaika wa Yeho-
va alivyokuwa amemwagiza,
naye akamchukua mke wake
na kwenda naye nyumbani.
25 Lakini hakufanya ngono
naye[m] mpaka alipozaa mwa-
na;[n] na Yosefu akamwita jina
lake Yesu.[o]

2 Baada ya Yesu kuzaliwa ka-
tika Bethlehemu[p] ya Yu-
dea siku za Mfalme Herode,[q]
tazama! wanajimu[r] kutoka se-
hemu za mashariki walikuja
Yerusalemu, **2** wakisema:
"Yuko wapi yule mfalme[s] wa
Wayahudi aliyezaliwa? Kwa
maana tuliiona nyota[a] yake
wakati tulipokuwa mashari-
ki, nasi tumekuja kumsuju-
dia." **3** Aliposikia hilo Mfa-
lme Herode akafadhaika, na
Yerusalemu yote pamoja naye;
4 na alipowakusanya pamoja
wakuu wa makuhani na waa-
ndishi wote wa watu akaanza
kuuliza habari kutoka kwao
juu ya ni wapi Kristo alipa-
swa kuzaliwa. **5** Wakamwa-
mbia: "Katika Bethlehemu[b] ya
Yudea; kwa maana hivi ndi-
yo ilivyoandikwa kupitia na-
bii, **6** 'Nawe, Ee Bethlehe-
mu[c] ya nchi ya Yuda, wewe si
jiji dogo zaidi kati ya magava-
na wa Yuda; kwa maana kuto-
ka kwako wewe atakuja mwe-
nye kuongoza,[d] atakayewachu-
nga[e] watu wangu, Israeli.'"

7 Ndipo Herode akawaita
wale wanajimu kwa siri na ku-
hakikisha kwa uangalifu kuto-
ka kwao wakati wa kuonekana
kwa ile nyota; **8** na, wakati
alipokuwa akiwatuma Bethle-
hemu, akasema: "Nendeni mka-
mtafute kwa uangalifu yule
mtoto mchanga, na mkiisha
kumpata nileteeni habari, ili
mimi vilevile nipate kwenda
na kumsujudia."[f] **9** Walipo-
kuwa wamemsikiliza mfalme,
waliondoka wakaenda; na, taza-
ma! nyota waliyokuwa wameo-
na wakati walipokuwa mashari-
ki[g] ikaenda mbele yao, mpa-
ka ikaja kutua juu ya mahali
alipokuwa yule mtoto mcha-
nga. **10** Walipoona ile nyota
walishangilia sana. **11** Nao
walipoingia ndani ya ile nyu-
mba wakamwona huyo mto-
to mchanga pamoja na Maria
mama yake, wakaanguka chini

SURA 1
a Kum 22:23
b Kum 24:1
c Lu 1:35
d Mt 1:25
Lu 1:31
Lu 2:21
e Lu 2:30
Ebr 7:25
f Mdo 5:31
g Yoh 1:29
Mdo 4:12
Efe 1:7
1Pe 2:24
h Isa 55:11
i Yak 5:10
2Pe 1:21
j Isa 7:14
k Isa 8:8
l Isa 8:10
m Lu 1:34
n Lu 2:7
o Lu 1:31
Lu 2:21

SURA 2
p Mik 5:2
Lu 2:4
q Lu 1:5
r Da 1:20
s Mwa 49:10
Mt 27:37

Safu ya 2
a Isa 47:13
Mt 2:9
b Yoh 7:42
c Mik 5:2
d Isa 44:28
e 2Sa 5:2
f Zb 37:12
Met 10:11
g Mt 2:2

na kumsujudia mtoto. Pia wa-
kafungua hazina zao na ku-
mtolea zawadi, dhahabu na uba-
ni na manemane. **12** Hata hi-
vyo, kwa sababu walipewa onyo
la kimungu[a] katika ndoto wa-
sirudi kwa Herode, wakaondo-
ka kwenda nchi yao kwa njia
nyingine.

13 Walipokuwa wamekwi-
sha kuondoka, tazama! malai-
ka wa Yehova[b] akamtokea Yo-
sefu katika ndoto, akisema:
"Simama, mchukue huyo mto-
to mchanga na mama yake
mkimbie kuingia Misri, mkae
huko mpaka nikupe agizo; kwa
maana Herode yuko karibu ku-
mtafuta huyo mtoto amwa-
ngamize." **14** Kwa hiyo aka-
simama na kuchukua pamo-
ja naye mtoto huyo mchanga
na mama yake wakati wa usi-
ku, akaondoka na kuingia Mi-
sri, **15** naye akakaa huko
mpaka kufa kwa Herode, ili li-
timizwe[c] lile lililosemwa na Ye-
hova kupitia nabii wake, akise-
ema: "Kutoka Misri[d] nilimwita
mwanangu."

16 Ndipo Herode, alipoona
ameshindwa akili na wale wa-
najimu, akaingiwa na gha-
dhabu kubwa, akatuma watu
na kuagiza wavulana wote ka-
tika Bethlehemu na katika
wilaya zake zote wauawe, ku-
anzia umri wa miaka miwi-
li kwenda chini, kulingana na
wakati aliokuwa amehakiki-
sha kwa uangalifu kutoka kwa
wale wanajimu.[e] **17** Ndipo li-
katimizwa lile lililosemwa ku-
pitia nabii Yeremia, akisema:
18 "Sauti ilisikiwa katika
Rama,[f] kulia na kuomboleza
kwingi; ni Raheli[g] aliyekuwa

SURA 2
a Mt 2:22
b Mt 1:20
Mt 2:19
c Mt 5:17
d Ho 11:1
e Mt 2:7
f Yer 31:15
Yer 31:16
g Mwa 35:19

Safu ya 2
a Mt 1:20
b Mt 2:12
c Mk 1:9
Lu 2:39
d Lu 2:51
Yoh 1:45
e Isa 11:1
Isa 53:2
Yer 23:5
Zek 3:8

SURA 3
f Mk 1:4
Yoh 1:6
g Mt 11:7
h Lu 3:3
i Mt 4:17
j Mk 1:2
Yoh 1:23
k Isa 40:3
l 2Fa 1:8
m Mk 1:6

akiwalilia watoto wake, naye
hakutaka kufarijiwa, kwa sa-
babu hawako tena."

19 Herode alipokuwa ame-
kufa, tazama! malaika wa Ye-
hova akamtokea Yosefu kati-
ka ndoto[a] huko Misri **20** naye
akasema: "Simama, mchukue
huyo mtoto mchanga na mama
yake, ushike njia na kuingia ka-
tika nchi ya Israeli, kwa maa-
na wale waliokuwa wakiitafu-
ta nafsi ya mtoto huyo wame-
kufa." **21** Kwa hiyo akasima-
ma na kumchukua huyo mtoto
mchanga na mama yake na
kuingia katika nchi ya Israe-
li. **22** Lakini aliposikia kwa-
mba Arkelao alikuwa akitawa-
la akiwa mfalme wa Yudea ba-
dala ya Herode baba yake, akao-
gopa kuondoka kwenda huko.
Zaidi ya hayo, kwa kuwa ali-
pewa onyo la kimungu kati-
ka ndoto,[b] akaondoka, akaingia
eneo la Galilaya,[c] **23** aka-
ja kukaa katika jiji linaloitwa
Nazareti,[d] ili lipate kutimi-
zwa lile lililosemwa kupitia ma-
nabii: "Yeye ataitwa Mnaza-
reti."[e]

3 Katika siku hizo Yohana
Mbatizaji[f] alikuja akihu-
biri katika nyika[g] ya Yudea,
2 akisema: "Tubuni,[h] kwa ma-
ana ufalme wa mbinguni ume-
karibia."[i] **3** Huyu, kwa kweli,
ndiye anayesemwa kupitia na-
bii Isaya[j] kwa maneno haya:
"Sikilizeni! Mtu fulani anapaa-
za sauti nyikani, 'Tayarisheni[k]
njia ya Yehova! Nyoosheni ba-
rabara zake.'" **4** Lakini Yo-
hana huyu mavazi yake yaliku-
wa ya manyoya ya ngamia[l] na
alikuwa na mshipi wa ngozi[m]
kiunoni mwake; nacho chaku-

la chake kilikuwa nzige[a] na
asali ya mwituni.[b] **5** Ndipo
Yerusalemu na Yudea yote na
nchi yote kandokando ya Yor-
dani zikamwendea, **6** naye
akawabatiza watu katika Mto
Yordani,[c] wakiungama waziwa-
zi dhambi zao.

7 Alipoona wengi wa Mafa-
risayo na Masadukayo[d] wakija
kwenye ubatizo, akawaambia:
"Ninyi uzao wa nyoka-vipiri,[e]
ni nani ambaye amewaonyesha
ninyi kuikimbia ghadhabu[f] ina-
yokuja? **8** Kwa hiyo basi za-
eni matunda yanayofaa toba;[g]
9 na msiseme moyoni mwenu,
'Abrahamu ndiye baba yetu.'[h]
Kwa maana ninawaambia ni-
nyi kwamba Mungu anaweza
kumwinulia Abrahamu[i] wato-
to kutoka katika mawe haya.
10 Tayari shoka[j] limewekwa
kwenye mzizi wa miti; basi,
kila mti usiozaa matunda ma-
zuri utakatwa[k] na kutupwa
ndani ya moto.[l] **11** Mimi ni-
nawabatiza ninyi kwa maji[m]
kwa sababu ya toba[n] yenu; laki-
ni yule anayekuja[o] nyuma ya-
ngu ana nguvu kuliko mimi,
ambaye viatu vyake mimi si-
stahili kuvivua.[p] Huyo atawa-
batiza ninyi kwa roho takatifu[q]
na kwa moto.[r] **12** Sepetu
yake ya kupepetea imo mko-
noni mwake, naye atausafisha
uwanja wake wa kupuria, na
kukusanya ngano yake katika
ghala[s] lakini makapi atayateke-
teza kwa moto[t] usioweza kuzi-
mwa."

13 Ndipo Yesu akaja kuto-
ka Galilaya[u] mpaka Yordani
kwa Yohana, kusudi ambati-
ze.[v] **14** Lakini Yohana akaja-
ribu kumzuia, akisema: "Mimi
ndiye ninayehitaji kubatizwa
na wewe, na je, wewe unaku-
ja kwangu?" **15** Yesu akaji-
bu, akamwambia: "Acha iwe hi-
yo, wakati huu, kwa maana
katika njia hiyo inafaa kwetu
kufanya yote yaliyo ya uadili-
fu."[a] Ndipo akaacha kumzuia.
16 Baada ya kubatizwa Yesu
akapanda mara moja kutoka
katika maji; na, tazama! mbi-
ngu zikafunguliwa,[b] naye aka-
ona roho ya Mungu ikishuka
kama njiwa,[c] ikija juu yake.[d]
17 Tazama! Kulikuwa pia na
sauti[e] kutoka mbinguni iliyo-
sema: "Huyu ni Mwanangu,[f]
mpendwa,[g] ambaye nimemku-
bali."[h]

4 Ndipo Yesu akaongozwa na
roho kuingia nyikani[i] ili ku-
jaribiwa[j] na Ibilisi. **2** Alipoku-
wa amefunga siku 40,[k] mchana
na usiku, akaona njaa. **3** Pia,
Mjaribu[l] akaja na kumwambia:
"Ikiwa wewe ni mwana wa Mu-
ngu,[m] yaambie mawe haya yawe
mikate." **4** Lakini akajibu na
kusema: "Imeandikwa, 'Mwa-
nadamu ataishi, si kwa mkate
tu, bali kwa kila neno linalotoka
katika kinywa cha Yehova.'"[n]

5 Ndipo Ibilisi akamchukua,
akaenda pamoja naye, na ku-
ingia katika lile jiji takatifu,[o]
naye akamsimamisha juu ya
mnara wa hekalu **6** na ku-
mwambia: "Ikiwa wewe ni mwa-
na wa Mungu, jitupe chini;[p] kwa
maana imeandikwa, 'Atawaagi-
za malaika zake kukuhusu
wewe, nao watakuchukua mi-
kononi mwao, ili usipate kamwe
kuugonga mguu wako juu ya
jiwe.'"[q] **7** Yesu akamwambia:

SURA 3

a Law 11:22
b 1Sa 14:27
Met 24:13
c Mk 1:5
Mk 1:9
d Mk 12:18
Lu 7:30
e Zb 58:4
Mt 12:34
f Mt 23:33
Lu 3:7
Lu 21:23
Ro 2:5
Ufu 6:17
g Mdo 26:20
h Yoh 8:33
Yoh 8:39
i Ro 4:12
j Lu 3:9
k Mt 7:19
Lu 13:6
l Yoh 15:6
m Yoh 1:33
Mdo 1:5
Mdo 11:16
n Mdo 13:24
Mdo 19:4
o Mt 11:3
Yoh 1:15
p Mk 1:7
Yoh 1:27
Mdo 13:25
q Yoh 1:33
Mdo 2:4
1Ko 12:13
r Lu 3:16
s Mt 13:30
t Yer 15:7
Mal 4:1
Lu 3:17
u Mk 1:9
v Lu 3:21

Safu ya 2

a Da 9:24
Mt 5:17
Ebr 10:9
b Eze 1:1
Mk 1:10
Lu 3:21
Mdo 7:56
c Yoh 1:32
d Isa 11:2
Lu 3:22
Lu 4:18
Mdo 10:38
e Yoh 12:28
f Mwa 22:2
Zb 2:7
Lu 9:35
g Mt 17:5
Lu 3:22
h Isa 42:1
Mt 12:18
2Pe 1:17

SURA 4

i Law 16:21
Mk 1:12
Lu 4:1
j Ebr 4:15
k Kut 34:28
Kum 9:9
1Fa 19:8
Mk 1:13
Lu 4:2
l 1Th 3:5

m Mt 27:40; Lu 4:3; n Kum 8:3; Lu 4:4; Yoh 4:34; o Ne 11:1; Isa 52:1; Mt 27:53; p Lu 4:9; q Zb 91:11; Zb 91:12; Lu 4:10; Lu 4:11.

"Tena imeandikwa, 'Usimjaribu
Yehova Mungu wako.'"[a]
8 Tena Ibilisi akamchukua,
akaenda pamoja naye kwenye
mlima mrefu isivyo kawaida,
na kumwonyesha falme zote za
ulimwengu[b] na utukufu wazo,
9 naye akamwambia: "Nitaku-
pa mambo yote haya[c] ukiangu-
ka chini na kunifanyia te-
ndo la ibada."[d] **10** Ndipo Yesu
akamwambia: "Nenda zako,
ni anamfukuza Shetani, amegawanyika na kujipinga mwenyewe; basi, ufalme wake utasimamaje? **27** Zaidi ya hayo, ikiwa mimi ninawafukuza roho waovu kwa nguvu za Beelzebuli,[a] wana wenu wanawafukuza kwa nguvu za nani? Ndiyo sababu wao watakuwa waamuzi wenu. **28** Lakini ikiwa mimi ninawatoa roho waovu kwa nguvu za roho ya Mungu, kwa kweli ufalme wa Mungu umewafikia ninyi ghafula.[b] **29** Au yeyote anawezaje kuivamia nyumba ya mtu mwenye nguvu na kukamata mali zake zinazoweza kuchukuliwa, asipomfunga kwanza mtu huyo mwenye nguvu? Na ndipo atakapoipora nyumba yake.[c] **30** Yeye asiyekuwa upande wangu ananipinga, naye asiyekusanya pamoja nami anatawanya.[d]

31 "Kwa hiyo mimi ninawaambia ninyi, Watu watasamehewa kila namna ya dhambi na kufuru, lakini hawatasamehewa kufuru juu ya roho.[e] **32** Kwa mfano, yeyote yule anayesema neno baya juu ya Mwana wa binadamu, atasamehewa;[f] lakini yeyote yule anayesema vibaya juu ya roho takatifu, hilo hatasamehewa, hapana, si katika mfumo huu wa mambo wala katika ule utakaokuja.[g]

33 "Ufanyeni mti uwe mzuri na matunda yake yawe mazuri au muufanye mti uoze na matunda yake yaoze; kwa maana kwa matunda yake mti hujulikana.[h] **34** Uzao wa nyoka-vipiri,[i] mnawezaje kusema mambo mema, wakati ninyi ni waovu?[a] Kwa maana kinywa kinasema kutokana na mambo yaliyojaa katika moyo.[b] **35** Mtu mwema hutoa mambo mema kutoka katika hazina yake njema,[c] lakini mtu mwovu hutoa mambo mabaya kutoka katika hazina yake mbaya.[d] **36** Ninawaambia ninyi kwamba kila neno lisilofaa ambalo watu husema, watatoa hesabu[e] juu yake katika Siku ya Hukumu; **37** kwa maana kwa maneno yako utatangazwa kuwa mwadilifu, na kwa maneno yako utahukumiwa."[f]

38 Ndipo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema: "Mwalimu, tunataka kuona ishara kutoka kwako."[g] **39** Akajibu, akawaambia: "Kizazi kiovu na chenye uzinzi[h] kinaendelea kutafuta ishara, lakini hakuna ishara kitakachopewa isipokuwa ishara ya nabii Yona.[i] **40** Kwa maana kama vile Yona[j] alivyokuwa katika tumbo la yule samaki mkubwa siku tatu mchana na usiku, ndivyo Mwana wa binadamu[k] atakavyokuwa katika moyo wa dunia[l] siku tatu mchana na usiku.[m] **41** Watu wa Ninawi watasimama katika hukumu pamoja na kizazi hiki[n] nao watakihukumu kuwa chenye hatia;[o] kwa sababu wao walitubu juu ya lile alilohubiri Yona,[p] lakini, tazama! mtu mkuu kuliko Yona yuko hapa. **42** Malkia wa kusini[q] atasimama katika hukumu pamoja na kizazi hiki naye atakihukumu kuwa chenye hatia; kwa sababu alikuja kutoka miisho ya dunia kuisikia hekima ya Sulemani,

SURA 12

a Mk 3:26
b Lu 11:20
1Yo 3:8
c Isa 49:24
Mk 3:27
Lu 11:22
1Yo 4:4
d Mk 9:40
Lu 9:50
e Mk 3:28
Mdo 7:51
Ebr 6:4
Ebr 6:6
1Yo 5:16
f Lu 7:34
Yoh 7:12
1Ti 1:13
g Mk 3:29
Lu 12:10
Ebr 10:26
h Mt 7:17
Lu 6:43
i Mt 3:7
Mt 23:33
Lu 3:7

Safu ya 2

a Ayu 14:4
b Mt 15:11
c Isa 32:8
d Mt 13:52
Lu 6:45
Yak 3:6
e Mhu 12:14
Ro 14:12
Yud 15
f Met 13:3
Lu 19:22
g Mt 16:1
Mk 8:11
Yoh 2:18
1Ko 1:22
h Isa 57:3
Mt 16:4
Mt 17:17
Mk 8:38
Yak 4:4
i Lu 11:29
j Yon 1:17
k Mt 27:63
l Mt 27:60
Efe 4:9
m Mt 16:21
Mt 17:23
Lu 24:46
n Lu 11:30
o Ro 2:27
p Yon 3:5
q 1Fa 10:1
2Nya 9:1

lakini, tazama! mtu mkuu kuliko Sulemani yuko hapa.[a]
43 "Wakati roho mchafu
anapomtoka mtu, hupita ka-
tika mahali pakavu akitafuta
mahali pa kupumzika, na hapa-
ti popote.[b] **44** Ndipo anasee-
ma, 'Nitarudi kwenye nyumba
yangu niliyoihama'; naye
anapofika anaikuta haijaka-
liwa lakini imefagiwa ikawa
safi na kupambwa. **45** Ndi-
po anaondoka na kwenda ku-
chukua roho tofauti saba walio
waovu zaidi kuliko yeye mwe-
nyewe,[c] na, baada ya kuingia
ndani, wao hukaa humo; na
hali ya mwisho ya mtu huyo
huwa mbaya zaidi kuliko ile ya
kwanza.[d] Hivyo ndivyo itaka-
vyokuwa pia kwa kizazi hiki ki-
ovu."[e]
46 Alipokuwa bado akise-
ma na umati, tazama! mama
yake na ndugu zake[f] waka-
ja na kusimama nje waki-
taka kusema naye. **47** Kwa
hiyo mtu fulani akamwambia:
"Tazama! Mama yako na ndugu
zako wamesimama nje, waki-
taka kusema nawe." **48** Aki-
mjibu huyo mwenye kumwa-
mbia, akasema: "Mama yangu
ni nani, na ndugu zangu ni
nani?"[g] **49** Naye akinyoosha
mkono wake kuelekea wanafu-
nzi wake, akasema: "Tazama!
Mama yangu na ndugu zangu![h]
50 Kwa maana yeyote yule
anayefanya mapenzi ya Baba
yangu aliye mbinguni, huyo
ndiye ndugu yangu, na dada ya-
ngu, na mama yangu."

13 Siku hiyo Yesu, akiisha
kuondoka katika ile nyu-
mba, alikuwa ameketi kando ya
bahari; **2** na umati mkubwa

SURA 12
a Mt 11:16
Mt 12:6
Lu 11:31
b Lu 11:24
c 1Pe 5:8
d Lu 11:26
Yoh 5:14
Ebr 6:4
Ebr 6:6
2Pe 2:20
e Mk 8:12
f Mt 13:55
Mk 3:31
Yoh 2:12
Mdo 1:14
1Ko 9:5
Ga 1:19
g Mk 3:33
h Mk 3:35
Yoh 14:23
Yoh 15:14
Yoh 20:17
Ro 8:29
Ebr 2:11

Safu ya 2

SURA 13
a Mk 4:1
b Mt 13:34
Mk 4:3
Lu 8:4
c Mt 13:19
Mk 4:4
Lu 8:5
d Mk 4:5
Lu 8:6
e Mt 13:20
Mt 13:21
Mk 4:6
f Mt 13:22
Mk 4:7
Mk 4:18
Mk 4:19
Lu 8:7
Ebr 6:8
g Yoh 15:16
h Mk 4:8
Lu 8:8
i Mt 11:15
j Mt 13:34
Mk 4:10
Lu 8:9
k 1Ko 2:10
Efe 1:9
Kol 1:26
l Lu 8:10
m Mt 25:29
n Mk 4:25
Lu 8:18
o Isa 6:10
Yer 5:21
Eze 12:2
Mk 4:12
Mk 8:18

ukamkusanyikia, hivi kwamba
akapanda ndani ya mashua na
kuketi,[a] na umati wote uliku-
wa umesimama pwani. **3** Ndi-
po akawaambia mambo mengi
kwa kutumia mifano, akisee-
ma: "Tazama! Mpandaji alie-
nda kupanda;[b] **4** naye alipo-
kuwa akipanda, mbegu fulani
zikaanguka kando ya barabara, na ndege wakaja na kuzila.[c]
5 Nyingine zikaanguka maha-
li penye miamba ambapo ha-
pakuwa na udongo mwingi, zi-
kachipuka mara moja kwa sa-
babu ya kutokuwa na udongo
wenye kina.[d] **6** Lakini jua lili-
pochomoza zikaungua, na kwa
sababu hazikuwa na mzizi zika-
nyauka.[e] **7** Nyingine, pia, zi-
kaanguka katikati ya miiba,
na ile miiba ikamea na kuzi-
songa.[f] **8** Bado nyingine zika-
anguka kwenye udongo mzuri
nazo zikaanza kuzaa matunda,[g]
hii mara 100, ile 60, ile nyingi-
ne 30.[h] **9** Yule aliye na masi-
kio na asikilize."[i]
10 Kwa hiyo wanafunzi wa-
kaja na kumwambia: "Kwa nini
unasema nao kwa kutumia
mifano?"[j] **11** Akajibu, akasee-
ma: "Ninyi mmepewa uwezo wa
kuzielewa siri takatifu[k] za ufa-
lme wa mbinguni, lakini wao
hawakupewa.[l] **12** Kwa maa-
na yeyote aliye na kitu, ataon-
gezewa naye atazidishiwa;[m] la-
kini yeyote ambaye hana, hata
kile alicho nacho kitachukuli-
wa.[n] **13** Ndiyo sababu nina-
sema nao kwa kutumia mifa-
no, kwa sababu, wakitazama,
wanatazama bure, na wakisi-
kia, wanasikia bure, wala ha-
waelewi;[o] **14** na unabii wa Isa-
ya unatimizwa kwao, ambao

unasema, ‘Kusikia, mtasikia la-
kini hamtaelewa maana yake;
na, kutazama, mtatazama laki-
ni hamtaona.[a] **15** Kwa maa-
na moyo wa watu hawa umeku-
wa mgumu, nao wamesikia
kwa masikio yao bila kuitikia,
nao wamefunga macho yao; ili
wasione kamwe kwa macho yao
na kusikia kwa masikio yao na
kuelewa maana kwa mioyo yao
na kugeuka, nami niwaponye.’[b]
16 “Hata hivyo, yenye fu-
raha ni macho[c] yenu kwa sa-
babu hayo yanaona, na masi-
kio yenu kwa sababu hayo ya-
nasikia. **17** Kwa maana kwa
kweli ninawaambia ninyi, Ma-
nabii[d] wengi na watu waadilifu
walitamani kuyaona mambo
mnayoyaona wala hawakuyaona,[e] na kuyasikia mambo mna-
yoyasikia wala hawakuyasi-
kia.[f]
18 “Basi, sikilizeni mfano wa
yule mtu aliyepanda.[g] **19** Ye-
yote anaposikia neno la ufa-
lme lakini haelewi maana yake,
yule mwovu[h] huja na kunya-
kua kile ambacho kimepa-
ndwa moyoni mwake; huyo
ndiye aliyepandwa kando ya
barabara. **20** Na yule aliye-
pandwa mahali penye miamba,
huyo ndiye anayelisikia neno
na kulipokea mara moja kwa
shangwe.[i] **21** Lakini hana
mzizi ndani yake bali huende-
lea kwa wakati fulani, na dhi-
ki au mateso vikiisha kuto-
kea kwa sababu ya lile neno
yeye hukwazika mara moja.[j]
22 Na yule aliyepandwa kati-
kati ya miiba, huyo ndiye ana-
yelisikia neno, lakini maha-
ngaiko ya mfumo huu wa ma-
mbo[k] na nguvu za udanganyi-
fu wa utajiri hulisonga neno,
naye huwa asiyezaa matunda.[a]
23 Na yule aliyepandwa juu ya
udongo mzuri, huyo ndiye ana-
yelisikia neno na kuelewa ma-
ana yake, ambaye kwa kweli
huzaa matunda na kutokeza,
huyu mara 100, yule 60, yule
mwingine 30.”[b]
24 Akawatolea mfano mwi-
ngine, akisema: “Ufalme wa
mbinguni umekuwa kama mtu
aliyepanda mbegu nzuri katika
shamba lake.[c] **25** Watu waki-
wa wamelala usingizi, adui yake
alikuja na kupanda magugu ka-
tikati ya ngano, naye akaondo-
ka. **26** Wakati jani lilipoota na
kuzaa matunda, magugu yalio-
nekana pia. **27** Kwa hiyo wa-
tumwa wa mwenye nyumba wa-
kaja na kumwambia, ‘Bwana, je,
hukupanda mbegu nzuri kati-
ka shamba lako?[d] Imekuwaje
basi lina magugu?’[e] **28** Aka-
waambia, ‘Adui, mtu fulani, ali-
fanya hivyo.’[f] Wakamwambia,
‘Basi, je, unataka twende kuya-
kusanya?’ **29** Akasema, ‘Ha-
pana; ili, mnapoyakusanya ma-
gugu, msije mkang’oa ngano
pamoja nayo. **30** Acheni zikue
pamoja mpaka wakati wa mavu-
no; na katika majira ya mavuno
nitawaambia wavunaji, Kwanza
kusanyeni magugu na kuyafu-
nga matita-matita ili kuyate-
keteza motoni,[g] ndipo ne-
ndeni mkusanye ngano ghalani
mwangu.’”[h]
31 Akawatolea mfano mwi-
ngine,[i] akisema: “Ufalme wa
mbinguni ni kama mbegu ya
haradali,[j] ambayo mtu alichu-
kua na kupanda katika sha-
mba lake; **32** ambayo, kwa
kweli, ndiyo mbegu ndogo

SURA 13

a Isa 6:9
Yoh 12:40
Mdo 28:26
Ro 11:8
2Ko 3:14

b Kum 32:28
Isa 44:18
Mk 8:17
Ebr 5:11

c Lu 10:23

d 1Pe 1:10

e Yoh 8:56
Efe 3:5

f Lu 10:24

g Mk 4:14
Lu 8:11

h Mk 4:15
Lu 8:12
1Pe 5:8

i Isa 58:2
Eze 33:31
Yoh 5:35

j Mt 24:10
Mk 4:17
Lu 8:13
2Ti 1:15

k Lu 12:22

Safu ya 2

a Mt 6:21
Mk 4:19
Mk 10:23
Lu 8:14
1Ti 6:9
2Ti 4:10

b Mk 4:20
Lu 8:15

c Mk 4:26

d Mt 13:38

e Mwa 1:11

f Mt 13:39

g Mt 3:12
Lu 3:17

h Ufu 14:15

i Mk 4:30

j Mt 17:20
Lu 13:19

zaidi kuliko zote, lakini ikiisha kukua huwa ndiyo kubwa zaidi kati ya mboga zote nayo huwa mti, hivi kwamba ndege wa mbinguni[a] huja na kupata makao katikati ya matawi yake."[b]

33 Akawaambia mfano mwingine: "Ufalme wa mbinguni ni kama chachu,[c] ambayo mwanamke alichukua na kuitia katika vipimo vikubwa vitatu vya unga, mpaka tonge lote likachacha."

34 Yesu aliuambia umati mambo yote hayo kwa mifano. Kwa kweli, hakuwa akisema nao bila mfano;[d] **35** ili litimizwe lililosemwa kupitia nabii aliyesema: "Nitakifungua kinywa changu kwa mifano, nitatangaza mambo yaliyofichwa tangu kuwekwa msingi."[e]

36 Ndipo baada ya kuuruhusu umati uende akaingia ndani ya nyumba. Na wanafunzi wake wakamjia na kusema: "Tueleze ule mfano wa magugu katika shamba." **37** Akajibu, akasema: "Mpandaji wa mbegu nzuri ni Mwana wa binadamu; **38** shamba ni ulimwengu;[f] nayo mbegu nzuri, hiyo ni wana wa ufalme; lakini magugu ni wana wa yule mwovu,[g] **39** na yule adui aliyepanda ni Ibilisi.[h] Yale mavuno[i] ni umalizio wa mfumo wa mambo,[j] na wavunaji ni malaika. **40** Kwa hiyo, kama vile magugu hukusanywa na kuteketezwa kwa moto, ndivyo itakavyokuwa katika umalizio wa mfumo wa mambo.[k] **41** Mwana wa binadamu atatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake vitu vyote ambavyo husababisha kukwazika[a] na watu wanaoasi sheria, **42** nao watawatupa ndani ya tanuru ya moto.[b] Humo ndimo watalia na kusaga meno yao.[c] **43** Wakati huo waadilifu watang'aa[d] kwa uangavu kama jua[e] katika ufalme wa Baba yao. Yule aliye na masikio na asikilize.[f]

44 "Ufalme wa mbinguni ni kama hazina iliyofichwa katika shamba, ambayo mtu aliipata na kuificha; na kwa sababu ya shangwe aliyo nayo, anaenda na kuuza[g] vitu alivyo navyo na kulinunua shamba hilo.[h]

45 "Tena ufalme wa mbinguni ni kama mwanabiashara msafiri anayetafuta lulu nzuri. **46** Akiisha kupata lulu moja ya thamani kubwa,[i] alienda zake na mara moja akauza vitu vyote alivyokuwa navyo na kuinunua.[j]

47 "Tena ufalme wa mbinguni ni kama wavu wa kukokota ulioshushwa ndani ya bahari na kukusanya samaki wa kila aina.[k] **48** Ulipojaa waliuvuta pwani na, baada ya kuketi, wakakusanya walio wazuri[l] ndani ya vyombo, lakini wasiofaa[m] wakawatupilia mbali. **49** Hivyo ndivyo itakavyokuwa katika umalizio wa mfumo wa mambo: malaika watatoka kwenda na kuwatenga waovu[n] kutoka katikati ya waadilifu[o] **50** nao watawatupa ndani ya tanuru ya moto. Humo ndimo watalia na kusaga meno yao.[p]

51 "Je, mmeelewa maana ya mambo haya yote?" Waka-

SURA 13

a Zb 104:12
Da 4:12
b Eze 17:23
c Lu 13:21
1Ko 5:6
Ga 5:9
d Mk 4:34
e Zb 78:2
Ro 16:25
1Ko 2:7
f Mt 24:14
Ro 10:18
Kol 1:6
g Yoh 8:44
h 1Yo 3:8
i Yoe 3:13
Ufu 14:15
j Ebr 9:26
k Mt 13:30

Safu ya 2

a Sef 1:3
1Ko 6:9
b Da 3:6
Mt 13:30
Mt 13:50
Ufu 21:8
c Zb 112:10
Mt 8:12
Lu 13:28
d Da 12:3
e Amu 5:31
2Sa 23:4
f Mk 4:23
Ufu 2:7
g Flp 3:7
h Isa 55:1
Ufu 3:18
i Flp 3:8
j Met 2:4
Met 8:18
k Mt 22:10
l Law 11:9
m Law 11:12
n Zb 1:5
o Mt 25:32
p Mt 8:12
Mt 22:13

mwambia: “Ndiyo.” **52** Ndipo akawaambia: “Ikiwa ni hivyo, kila mfundishaji wa watu
wote, anapofundishwa kuhusiana na ufalme wa mbinguni,[a]
ni kama mtu, mwenye nyumba, ambaye hutoa katika hazina yake vitu vipya na vya zamani.”[b]

53 Sasa Yesu alipokuwa amemaliza mifano hiyo alitoka na
kupita katikati ya nchi. **54** Na baada ya kuingia eneo lake la
nyumbani[c] akaanza kuwafundisha katika sinagogi lao,[d] hivi
kwamba wakastaajabu na kusema: “Mtu huyu alipata wapi
hekima hii na kazi hizi zenye nguvu? **55** Je, huyu si mwana wa yule seremala?[e] Je, mama
yake haitwi Maria, na ndugu zake Yakobo na Yosefu na Simoni na Yuda? **56** Na dada zake,
je, wote hawako pamoja nasi?[f] Basi, mtu huyu alipata wapi
mambo haya yote?”[g] **57** Kwa hiyo wakaanza kukwazika kwa
sababu yake.[h] Lakini Yesu akawaambia: “Nabii hakosi kuheshimiwa ila katika eneo lake
la nyumbani na katika nyumba yake mwenyewe.”[i] **58** Naye
hakufanya kazi nyingi zenye nguvu huko kwa sababu ya ukosefu wao wa imani.[j]

14 Wakati huo Herode, mtawala wa wilaya, akasikia habari juu ya Yesu[k] **2** na
kuwaambia watumishi wake:
“Huyu ndiye Yohana Mbatizaji.
Alifufuliwa kutoka kwa wafu,
na ndiyo sababu anatenda kazi
zenye nguvu.”[l] **3** Kwa maana
Herode alikuwa amemkamata Yohana, akamfunga na
kumweka gerezani kwa sababu
ya Herodia mke wa Filipo ndugu yake.[a] **4** Kwa maana Yohana alikuwa akimwambia: “Si
halali wewe kuwa na mwanamke huyo.”[b] **5** Hata hivyo,
ijapokuwa alitaka kumuua, aliuogopa umati, kwa sababu wa-
limwona kuwa nabii.[c] **6** Lakini sikukuu ya kuzaliwa[d] kwa
Herode ilipokuwa ikisherehekewa binti ya Herodia alicheza dansi na kumpendeza sana
Herode **7** hivi kwamba akaahidi kwa kiapo kumpa chochote kile ambacho angeomba.[e]
8 Ndipo yeye, chini ya mwelekezo wa mama yake, akasema: “Nipe hapa juu ya sahani kichwa cha Yohana Mbatizaji.”[f] **9** Ajapokuwa na huzuni, mfalme kwa kufikiria viapo
vyake na kwa ajili ya wale wenye kuketi pamoja naye akaamuru apewe hicho;[g] **10** naye
akatuma watu wakamkate Yohana kichwa huko gerezani.
11 Na kichwa chake kikaletwa juu ya sahani na yule mwanamwali akapewa, naye akampelekea mama yake.[h] **12** Mwishowe wanafunzi wake wakaja na kuiondoa maiti na kumzika[i] nao wakaja na kumjulisha
Yesu. **13** Aliposikia hilo Yesu akaondoka hapo kwa mashua
kwenda mahali pasipo na watu ili awe peke yake;[j] lakini umati, uliposikia hilo, ukamfuata
kwa miguu kutoka katika majiji.

14 Basi alipotokea akaona umati mkubwa; naye akawa-
sikitikia,[k] akaponya wagonjwa
wao.[l] **15** Lakini jioni ilipo-
fika wanafunzi wake wakamjia na kusema: “Mahali hapa
hapana watu na saa tayari
imesonga sana; acha umati

SURA 13
a 1Ko 4:1
b Mt 12:35
Lu 6:45
c Mt 2:23
Mk 6:1
d Lu 4:16
e Mk 6:3
Lu 3:23
Lu 4:22
Yoh 6:42
f Mt 12:46
Yoh 2:12
Mdo 1:14
1Ko 9:5
Ga 1:19
g Yoh 7:15
h Mt 15:12
1Pe 2:8
i Yer 11:21
Lu 4:24
Yoh 4:44
j Mk 6:6

SURA 14
k Mk 6:14
Lu 9:7
Mdo 4:27
l Mt 16:14
Mk 6:14
Mk 6:16

Safu ya 2
a Mt 4:12
Mk 6:17
Lu 3:19
b Law 18:16
Law 20:21
Mt 19:9
c Mt 21:26
Mk 6:20
Lu 1:76
Lu 20:6
d Mwa 40:20
e 1Sa 14:28
1Sa 25:22
Mk 6:22
f Mk 6:24
g Mk 6:26
h Mt 17:12
Mk 6:28
i Mk 6:29
Mdo 8:2
j Mk 6:31
Lu 9:10
k Mt 9:36
Mt 15:32
Mk 1:41
Lu 7:13
Ebr 2:17
Ebr 5:2
l Lu 9:11

waende zao, ili wapate kwenda vijijini na kujinunulia chakula."[a] **16** Hata hivyo, Yesu
akawaambia: "Si lazima waondoke: Ninyi wapeni chakula."[b] **17** Wakamwambia: "Hatuna kitu hapa ila mikate mitano na samaki wawili."[c]
18 akasema: "Vileteni hapa."
19 Halafu akauamuru umati uketi kwenye majani naye akachukua ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni, akatoa baraka[d] na, baada ya kuimega ile mikate, akawagawia wanafunzi, nao wanafunzi wakaugawia ule umati.[e] **20** Kwa hiyo wote wakala wakashiba, nao wakaokota vipande vilivyobaki, vikapu kumi na viwili vilivyojaa.[f] **21** Na bado wale waliokula walikuwa wanaume karibu elfu tano, bila kuhesabu wanawake na watoto wachanga.[g] **22** Ndipo, bila kukawia, akawaagiza wanafunzi wake waipande mashua na kumtangulia kwenda upande ule mwingine, huku akiwaruhusu umati waende zao.[h]

23 Mwishowe, baada ya kuwaruhusu umati waende zao, akapanda mlimani akiwa peke yake ili kusali.[i] Ingawa ilikuwa jioni, alikuwa huko peke yake.
24 Kufikia sasa mashua ilikuwa mamia mengi ya meta mbali na nchi kavu, ikitaabishwa sana na mawimbi,[j] kwa sababu upepo ulikuwa ukivuma kinyume chao. **25** Lakini katika kipindi cha kesha la nne la usiku akawajia, akitembea juu ya bahari.[k] **26** Walipomwona akitembea juu ya bahari, wanafunzi wakahangaika,

SURA 14
a Lu 9:12
b Mk 6:37
c Lu 9:13
Yoh 6:9
d Mt 15:36
Mk 6:41
Lu 9:16
e Mk 6:39
Yoh 6:10
f 2Fa 4:44
Mk 8:8
Lu 9:17
Yoh 6:12
g Mk 6:44
Lu 9:14
Yoh 6:10
h Mk 6:45
Yoh 6:15
i Mk 6:46
Lu 6:12
Lu 9:18
j Yoh 6:18
k Mk 6:48
Yoh 6:19

Safu ya 2
a Lu 24:37
b Mk 6:50
Yoh 6:20
Mdo 23:11
c Yoh 21:7
d Mt 6:30
Mt 8:26
Mt 28:17
Yak 1:6
e Mt 16:16
Yoh 6:69
f Mk 6:53
Yoh 6:21
g Mk 6:56
h Law 6:27
Hes 15:38
Mt 9:21
Mk 3:10
Lu 6:19

SURA 15
i Mk 7:1
j Mk 7:2
Lu 11:38
Yoh 2:6

wakisema: "Ni mzuka!"[a] Nao wakapaaza sauti katika woga wao. **27** Lakini Yesu akasema nao mara moja kwa maneno haya: "Jipeni moyo, ni mimi;[b] msiogope." **28** Petro akajibu, akamwambia: "Bwana, ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji." **29** Akasema: "Njoo!" Petro akashuka mara moja kutoka kwenye mashua,[c] akatembea juu ya maji na kumwendea Yesu. **30** Lakini akiitazama ile dhoruba ya upepo, akaogopa na, alipoanza kuzama, akapaaza sauti: "Bwana, niokoe!" **31** Mara moja Yesu akaunyoosha mkono wake, akamshika na kumwambia: "Wewe mwenye imani kidogo, kwa nini umekuwa na shaka?"[d] **32** Na baada ya kupanda katika mashua, dhoruba ya upepo ikapunguka.
33 Ndipo wale waliokuwa ndani ya mashua wakamsujudia, wakisema: "Wewe kwa kweli ni Mwana wa Mungu."[e] **34** Nao wakavuka na kuja kwenye nchi kavu katika Genesareti.[f]

35 Walipomtambua, watu wa mahali hapo wakapeleka habari katika nchi yote hiyo jirani, na watu wakamletea wale wote waliokuwa wagonjwa.[g]
36 Nao wakaanza kumsihi ili wapate kuugusa tu upindo wa vazi lake la nje;[h] na wale wote waliougusa wakapona kabisa.

15 Ndipo Mafarisayo na waandishi kutoka Yerusalemu[i] wakamjia Yesu, wakasema: **2** "Kwa nini wanafunzi wako huvunja mapokeo ya watu wa zamani? Kwa mfano, hawanawi mikono yao kabla ya kula."[j]

3 Akajibu, akawaambia:
"Kwa nini ninyi pia huvunja
amri ya Mungu kwa sababu ya
mapokeo yenu?[a] **4** Kwa mfa-
no, Mungu alisema, 'Mheshimu
baba yako na mama yako';[b]
na, 'Yule anayemtukana baba
yake au mama yake na afe.'[c]
5 Lakini ninyi husema, 'Yeyo-
te anayemwambia baba yake
au mama yake: "Chochote ni-
licho nacho unachoweza ku-
faidika nacho kutoka kwa-
ngu ni zawadi iliyowekwa wa-
kfu kwa Mungu," **6** asimhe-
shimu baba yake hata kidogo.'[d]
Na kwa hiyo ninyi mmelibatili-
sha neno la Mungu kwa saba-
bu ya mapokeo yenu.[e] **7** Ninyi
wanafiki,[f] Isaya[g] kwa kufaa ali-
toa unabii juu yenu, aliposema,
8 'Watu hawa huniheshimu
kwa midomo yao, bali moyo
wao umepelekwa mbali nami.[h]
9 Wao huniabudu bure, kwa
sababu wao hufundisha amri
za wanadamu kuwa mafu-
ndisho.'"[i] **10** Ndipo akauita
umati karibu na kuwaambia:
"Sikilizeni na mwelewe maa-
na:[j] **11** Mtu hatiwi unajisi na
kile kinachoingia ndani ya ki-
nywa chake; bali kinachotoka
katika kinywa chake ndicho
humtia unajisi."[k]
12 Ndipo wanafunzi waka-
ja na kumwambia: "Je, unajua
kwamba Mafarisayo walikwa-
zika waliposikia uliyosema?"[l]
13 Akajibu, akasema: "Kila
mmea ambao Baba yangu wa
mbinguni hakuupanda utang'o-
lewa.[m] **14** Waacheni. Wao ni
viongozi vipofu. Basi, ikiwa
kipofu anamwongoza kipofu,
wote wawili wataanguka nda-
ni ya shimo."[n] **15** Petro aka-
mjibu, akamwambia: "Tufafa-
nulie mfano huo."[a] **16** Ndipo
akasema: "Je, ninyi pia bado
hamwelewi?[b] **17** Je, hamjui
kwamba kila kitu kinachoin-
gia katika kinywa hupita nda-
ni ya matumbo na huondole-
wa na kuingia katika shimo la
choo? **18** Hata hivyo, mambo
yanayotoka katika kinywa hu-
toka moyoni, na mambo hayo
humtia mtu unajisi.[c] **19** Kwa
mfano, mawazo mabaya hutoka
moyoni,[d] mauaji, uzinzi, ua-
sherati, wizi, ushuhuda wa
uwongo, makufuru.[e] **20** Hayo
ndiyo mambo yanayomtia mtu
unajisi; lakini kula bila kuna-
wa mikono hakumtii mtu unaji-
si."[f]
21 Sasa Yesu akatoka hapo,
akaondoka na kuingia kati-
ka sehemu za Tiro na Sido-
ni,[g] **22** Na, tazama! mwana-
mke Mfoinike[h] kutoka katika
maeneo hayo akatoka na ku-
paaza sauti kubwa, akisema:
"Uwe na rehema juu yangu,[i]
Bwana, Mwana wa Daudi. Bi-
nti yangu anasumbuliwa sana
na roho mwovu." **23** Laki-
ni yeye hakumjibu neno lolo-
te mwanamke huyo. Kwa hiyo
wanafunzi wake wakaja na ku-
anza kumwomba: "Mwache ae-
nde zake; kwa sababu anaende-
lea kupaaza sauti akitufuata
nyuma." **24** Akajibu, akasem-
a: "Sikutumwa kwa wowo-
te ila kwa kondoo waliopo-
tea wa nyumba ya Israeli."[j]
25 Mwanamke huyo alipokuja
akaanza kumsujudia, akisema:
"Bwana, nisaidie!"[k] **26** Akaji-
bu, akasema: "Si sawa kuuchu-
kua mkate wa watoto na kuwa-
tupia mbwa wadogo." **27** Yeye

SURA 15
a Mt 15:9
Mk 7:8
Kol 2:8
Tit 1:14
b Kut 20:12
Kum 5:16
Efe 6:2
c Kut 21:17
Law 20:9
Kum 27:16
Mk 7:10
d Mk 7:12
e Mk 7:13
f Mt 23:13
g Mk 7:6
h Isa 29:13
i Zb 78:37
Eze 33:31
Mk 7:7
Kol 2:22
j Mk 7:14
k Mt 12:34
Mk 7:15
Efe 4:29
1Ti 4:4
Yak 3:6
l Mk 7:17
m Yoh 15:6
Mdo 5:38
n Isa 9:16
Mal 2:8
Mt 23:16
Lu 6:39
Yoh 9:40

Safu ya 2
a Mt 13:36
Mk 4:10
Lu 8:9
b Mk 7:18
c Zb 5:9
Mk 7:20
Ro 3:13
d Mwa 8:21
Kum 15:9
Met 6:14
Yer 17:9
Ro 1:28
e Mk 7:21
Ga 5:19
f Mk 7:23
g Mk 7:24
h 1Fa 17:9
Mk 7:26
Lu 4:26
i Mt 20:30
j Isa 53:6
Mt 10:6
Mdo 3:26
Mdo 13:46
Ro 15:8
k Mk 7:26

akasema: "Ndiyo, Bwana; lakini kwa kweli hao mbwa wadogo
hula sehemu ya makombo yana-
yoanguka kutoka kwenye meza
ya mabwana zao."[a] **28** Ndipo
Yesu akamjibu, akasema: "Ewe
mwanamke, imani yako ni ku-
bwa; acha itendeke kwako kama
unavyotaka." Na binti yake aka-
ponywa tangu saa hiyo na kue-
ndelea.[b]
29 Kisha kutoka hapo, Yesu
akavuka nchi, akaja karibu na
bahari ya Galilaya,[c] na, baada
ya kupanda mlimani,[d] akaketi
huko. **30** Ndipo umati mku-
bwa ukamkaribia, wakiwa pa-
moja na watu waliokuwa vi-
wete, vilema, vipofu, mabubu,
na wengine wengi, nao waka-
waweka miguuni pake, naye
akawaponya;[e] **31** hivi kwa-
mba umati wakashangaa wa-
lipoona mabubu wakisema na
viwete wakitembea na vipo-
fu wakiona, nao wakamtukuza
Mungu wa Israeli.[f]
32 Lakini Yesu akawaita
wanafunzi wake na kusema:[g]
"Ninausikitikia[h] umati, kwa
sababu tayari wamekaa pamo-
ja nami siku tatu nao hawa-
na chakula; nami sitaki ku-
waacha waende zao wakiwa
wamefunga. Huenda wakazi-
mia barabarani." **33** Hata
hivyo, wanafunzi wakamwa-
mbia: "Katika mahali hapa
pasipo na watu tutapata wapi
mikate ya kutosha kuushi-
bisha umati huu mkubwa?"[i]
34 Ndipo Yesu akawaambia:
"Mna mikate mingapi?" Waka-
sema: "Saba, na samaki wado-
go wachache." **35** Kwa hiyo,
baada ya kuuagiza umati uketi
chini, **36** akachukua ile mi-

SURA 15
a Mk 7:28
b Mk 7:29
Yoh 4:53
c Mk 7:31
d Mt 5:1
e Isa 35:5
Mt 19:2
Mk 3:10
Mk 7:32
f Mt 9:33
Mk 7:37
g Mk 8:1
h Mt 14:14
Mk 6:34
i Hes 11:22
2Fa 4:43
Mk 8:4

Safu ya 2
a Kum 8:10
1Sa 9:13
Mt 14:19
Mk 8:6
b Mt 16:10
Mk 8:8
c Mk 8:10

SURA 16
d Mt 12:38
e Mk 8:11
Lu 11:16
1Ko 1:22
f Isa 7:14
Mik 5:2
Lu 12:54
g Mk 8:12
h Yon 1:17
i Mt 12:39
Lu 11:29
j Mk 8:13
Mk 8:14
k Mt 24:4
Mk 8:15
Lu 12:1
Ro 16:17
Kol 2:8

kate saba na wale samaki na,
baada ya kushukuru, akamega
na kuanza kuwagawia wanafu-
nzi, nao wanafunzi wakawaga-
wia umati.[a] **37** Na wote wa-
kala na kushiba, nao wakaoko-
ta vipande vilivyobaki, vikapu
saba vya chakula vilivyojaa.[b]
38 Na bado wale waliokula wa-
likuwa wanaume elfu nne, bila
kuhesabu wanawake na wato-
to wachanga. **39** Mwishowe,
baada ya kuacha umati waende
zao, akaingia katika mashua
na kwenda katika maeneo ya
Magadani.[c]
16 Ndipo Mafarisayo[d] na Ma-
sadukayo wakamkaribia
na, ili kumjaribu, wakamwo-
mba awaonyeshe ishara kutoka
mbinguni.[e] **2** Akajibu, akawa-
ambia: "[[Inapokuwa jioni ni-
nyi huwa na desturi ya kusema,
'Kutakuwa na hali nzuri
ya hewa, kwa maana anga ni
jekundu'; **3** na asubuhi, 'Ku-
takuwa na baridi kali, na mvua
leo, kwa maana anga ni jeku-
ndu, na lenye mawingu ma-
zito.' Mnajua jinsi ya kufasi-
ri kuonekana kwa anga, lakini
ishara za nyakati hamwezi ku-
zifasiri.]][f] **4** Kizazi kiovu na
chenye uzinzi kinaendelea ku-
tafuta ishara, lakini hakuna
ishara ambayo kitapewa[g] ila ile
ishara ya Yona."[h] Ndipo akawa-
acha, akaenda zake.[i]
5 Sasa wanafunzi wakavu-
ka mpaka ule upande mwi-
ngine na kusahau kuichukua
mikate.[j] **6** Yesu akawaambia:
"Endeleeni kufungua macho
yenu na kujihadhari na cha-
chu ya Mafarisayo na Masa-
dukayo."[k] **7** Kwa hiyo waka-
anza kujadiliana, wakisema:

"Hatukuchukua mikate yoyote." **8** Akijua hilo, Yesu akasema: "Kwa nini mnajadiliana, kwa sababu hamna mikate, ninyi wenye imani kidogo?[a] **9** Je, bado hamwelewi maana, au je, hamkumbuki ile mikate mitano katika kisa cha wale elfu tano na ni vikapu vingapi mlivyookota?[b] **10** Au ile mikate saba katika kisa cha wale elfu nne na ni vikapu vingapi vya chakula mlivyookota?[c] **11** Imekuwaje kwamba hamfahamu kwamba sikuongea nanyi juu ya mikate? Bali jihadharini na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo."[d] **12** Ndipo wakafahamu kwamba alisema juu ya kujihadhari, si na chachu ya ile mikate, bali na mafundisho[e] ya Mafarisayo na Masadukayo.

13 Sasa alipoingia katika sehemu za Kaisaria Filipi, Yesu akaanza kuwauliza wanafunzi wake: "Watu wanasema Mwana wa binadamu ni nani?"[f] **14** Wakasema: "Baadhi yao husema Yohana Mbatizaji,[g] wengine Eliya,[h] na wengine bado Yeremia au mmoja wa manabii." **15** Akawaambia: "Ingawa hivyo, ninyi mnasema mimi ni nani?"[i] **16** Simoni Petro akajibu, akasema: "Wewe ndiye Kristo,[j] Mwana wa Mungu aliye hai."[k] **17** Yesu akajibu, akamwambia: "Mwenye furaha ni wewe, Simoni mwana wa Yona, kwa sababu nyama na damu havikukufunulia hilo, bali Baba yangu aliye mbinguni ndiye aliyekufunulia.[l] **18** Pia, ninakuambia, Wewe ni Petro,[m] na juu ya mwamba huu[n] nitajenga kutaniko langu, na malango ya Kaburi*[a] hayatalizidi nguvu.[b] **19** Nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni, na lolote utakalofunga duniani litakuwa jambo lililofungwa mbinguni, na lolote utakalofungua duniani litakuwa jambo lililofunguliwa mbinguni."[c] **20** Ndipo akawaagiza wanafunzi kwa kusisitiza wasimwambie yeyote kwamba yeye ni Kristo.[d]

21 Tangu wakati huo na kuendelea Yesu Kristo akaanza kuwaonyesha wanafunzi wake kwamba ni lazima aende Yerusalemu na kupatwa na mambo mengi kutoka kwa wanaume wazee na wakuu wa makuhani na waandishi, na kuuawa, na siku ya tatu afufuliwe.[e] **22** Ndipo Petro akamchukua kando na kuanza kumkemea, akisema: "Jitendee kwa fadhili, Bwana; wewe hutapatwa hata kidogo na jambo hili."[f] **23** Lakini akamgeuzia mgongo wake, akamwambia Petro: "Nenda nyuma yangu, Shetani![g] Wewe ni kikwazo kwangu, kwa sababu wewe unafikiri, si fikira za Mungu,[h] bali za wanadamu."

24 Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi wake: "Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe na kuuchukua mti wake wa mateso na kunifuata sikuzote.[i] **25** Kwa maana yeyote yule anayetaka kuiokoa nafsi yake ataipoteza; lakini yeyote yule anayeipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataipata.[j] **26** Kwa maana mtu atapata faida gani akiupata ulimwengu wote lakini aipoteze nafsi

SURA 16
a Mt 8:26
Mk 8:17
b Mt 14:17
Mk 8:19
c Mt 15:34
Mk 8:20
d Law 2:11
Law 6:17
Mk 8:21
Lu 12:1
e Mt 15:3
f Mk 8:27
Lu 9:18
g Mt 14:2
Lu 9:7
h Yoh 1:25
i Mk 8:29
Lu 9:20
j Yoh 1:41
Yoh 4:25
Yoh 11:27
k Zb 2:7
Mt 14:33
Mdo 9:20
Ebr 1:2
1Yo 4:15
l Mt 11:27
Mt 17:5
m Yoh 1:42
n Ro 9:33
1Ko 3:11
1Ko 10:4
Efe 2:20
1Pe 2:8

Safu ya 2
a Isa 28:18
b Ufu 1:18
c Mt 18:18
Yoh 20:23
d Mk 8:30
Lu 9:21
e Zb 16:10
Isa 53:12
Mt 17:23
Mt 20:19
Mk 8:31
Lu 9:22
Lu 24:46
1Ko 15:4
f Mk 8:32
g Mt 4:10
h 1Ko 2:11
i Mt 10:38
Mk 8:34
Lu 9:23
Lu 14:27
j Lu 17:33
Yoh 12:25
Ufu 12:11

Mt 16:18* Hadesi. Tazama Nyongeza 4.

yake?[a] au mtu atatoa nini ili
aipate[b] nafsi yake? **27** Kwa
maana Mwana wa binadamu
anakusudiwa kuja katika utu-
kufu wa Baba yake pamoja na
malaika zake, na ndipo ata-
kapomlipa kila mmoja kuli-
ngana na mwenendo wake.[c]
28 Kwa kweli ninawaambia
ninyi kwamba kuna baadhi
ya wale wanaosimama hapa
ambao hawataonja kifo ka-
mwe mpaka kwanza wamwone
Mwana wa binadamu akija ka-
tika ufalme wake."[d]

17 Siku sita baadaye Yesu ali-
wachukua Petro na Yako-
bo na Yohana ndugu yake aka-
wapandisha katika mlima mre-
fu wakiwa peke yao.[e] **2** Sura
yake ikageuka mbele yao, na uso
wake ukang'aa kama jua,[f] na ma-
vazi yake ya nje yakang'aa kama
nuru.[g] **3** Na, tazama! Musa
na Eliya wakawatokea, wakio-
ngea naye.[h] **4** Petro akamjibu,
akamwambia Yesu: "Bwana, ni
vizuri kwetu kuwa hapa. Ukita-
ka, nitasimamisha mahema ma-
tatu hapa, moja lako na moja la
Musa na moja la Eliya."[i] **5** Ali-
pokuwa bado akisema, taza-
ma! wingu jangavu liliwafuni-
ka, na, tazama! kulikuwa na sa-
uti kutoka katika lile wingu,
ikisema: "Huyu ni Mwanangu,
mpendwa, ambaye nimemkuba-
li;[j] msikilizeni."[k] **6** Waliposi-
kia hilo wanafunzi wakaangu-
ka kifudifudi na kuogopa sana.[l]
7 Ndipo Yesu akaja karibu, aka-
wagusa, na kusema: "Simame-
ni na msiogope."[m] **8** Walipoi-
nua macho yao, hawakumwona
yeyote ila Yesu mwenyewe tu.[n]
9 Na walipokuwa wakishuka
kutoka mlimani, Yesu akawaa-
muru, akisema: "Msimwambie
mtu yeyote maono hayo mpaka
Mwana wa binadamu afufuliwe
kutoka kwa wafu."[a]
10 Hata hivyo, wanafunzi
wakamuuliza swali hili: "Basi,
kwa nini waandishi husema
kwamba lazima Eliya aje kwa-
nza?"[b] **11** Akajibu, akasema:
"Eliya, kwa kweli, anakuja
naye atarudisha mambo yote.[c]
12 Hata hivyo, mimi ninawaa-
mbia ninyi kwamba tayari Eli-
ya amekuja nao hawakumta-
mbua bali walimtendea ma-
mbo waliyotaka. Katika njia
hiyo pia Mwana wa binadamu
atateseka mikononi mwao."[d]
13 Ndipo wanafunzi wakafa-
hamu kwamba alikuwa aki-
waambia juu ya Yohana Mba-
tizaji.[e]
14 Nao walipofika mahali
ulipokuwa umati,[f] mtu fula-
ni akamkaribia, akampigia ma-
goti, na kusema: **15** "Bwana,
uwe na rehema juu ya mwa-
nangu, kwa sababu ana kifa-
fa na ni mgonjwa, kwa maana
yeye huanguka ndani ya moto
na ndani ya maji mara nyingi;[g]
16 nami nilimleta kwa wana-
funzi wako, lakini hawakuwe-
za kumponya."[h] **17** Yesu aka-
jibu, akasema: "Enyi kizazi ki-
sicho na imani na kilichopoto-
ka,[i] nitaendelea kuwa pamoja
nanyi mpaka wakati gani? Ni-
tawavumilia ninyi mpaka wa-
kati gani? Mleteni hapa."
18 Ndipo Yesu akamkemea,
na huyo roho mwovu akamto-
ka;[j] naye mvulana akapona ta-
ngu saa hiyo.[k] **19** Ndipo wa-
nafunzi wakamjia Yesu fara-
ghani na kusema: "Kwa nini
sisi hatukuweza kumfukuza?"[l]

SURA 16
a Mk 8:36
b Zb 49:8
c Zb 62:12
Met 24:12
Ro 2:6
2Ko 5:10
1Pe 1:17
d Mt 10:23
Mt 17:2
Mk 9:1

SURA 17
e Mk 9:2
Lu 9:28
2Pe 1:18
f Kut 34:29
g 2Pe 1:17
Ufu 1:16
h Mk 9:4
i Mk 9:5
j Zb 2:7
Isa 42:1
Mt 3:17
Lu 9:35
k Kum 18:15
Mdo 3:23
Ebr 2:3
l Mk 9:6
m Ufu 1:17
n Mk 9:8

Safu ya 2
a Mt 16:20
Mk 9:9
Lu 9:36
b Mt 11:14
c Isa 40:3
Mal 3:1
Mal 4:5
Lu 1:17
d Mt 16:21
Mk 9:13
Lu 23:25
e Lu 1:17
f Lu 9:37
g Mk 9:17
h Lu 9:40
i Kum 32:5
Kum 32:20
Flp 2:15
j Mk 9:25
k Mt 8:13
Mt 9:22
Mt 15:28
Yoh 4:52
l Mk 9:28

20 Akawaambia: "Ni kwa sababu ya imani yenu kidogo,
kwa maana kwa kweli ninawaambia, Mkiwa na imani inayotoshana na mbegu ya haradali,
mtauambia mlima huu, 'Ondoka hapa uende pale,' nao utaondoka, na hakuna jambo litakalowashinda."[a] **21** ——

22 Walipokuwa wamekusanyika pamoja katika Galilaya,
Yesu akawaambia: "Mwana wa binadamu atasalitiwa mikononi mwa watu,[b] **23** nao watamuua, na siku ya tatu atafufuliwa."[c] Kwa hiyo wakahuzunika sana.[d]

24 Walipofika Kapernaumu
watu wanaokusanya kodi ya drakma mbili wakamkaribia Petro na kusema: "Je, mwalimu wenu halipi kodi ya drakma mbili?"[e] **25** Akasema: "Analipa." Hata hivyo, alipoingia ndani ya nyumba Yesu akamtangulia kusema: "Unaonaje, Simoni? Wafalme wa dunia hupokea ushuru au kodi ya kichwa kutoka kwa nani? Kutoka kwa wana wao au kutoka kwa wageni?" **26** Aliposema: "Kutoka kwa wageni," Yesu akamwambia: "Basi, kwa kweli wana hawalipi kodi. **27** Lakini ili tusiwakwaze,[f] wewe nenda baharini, utupe ndoano, na kuchukua samaki wa kwanza atakayetokea, ukifungue kinywa chake, nawe utapata sarafu ya stateri. Ichukue na uwape kwa ajili yangu na kwa ajili yako."[g]

18 Katika saa hiyo wanafunzi wakamkaribia Yesu
na kusema: "Ni nani kwa kweli aliye mkuu zaidi katika ufalme wa mbinguni?"[h] **2** Basi, akamwita mtoto mchanga, akamweka katikati yao[a] **3** na kusema: "Kwa kweli ninawaambia ninyi, Msipogeuka na kuwa kama watoto wachanga,[b] hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.[c] **4** Basi, yeyote atakayejinyenyekeza[d] mwenyewe kama mtoto huyu mchanga ndiye aliye mkuu zaidi katika ufalme wa mbinguni;[e] **5** na yeyote yule anayempokea mtoto mchanga kama huyu kwa msingi wa jina langu ananipokea mimi pia.[f] **6** Lakini yeyote anayemkwaza mmoja wa hawa wadogo wanaoniamini, ingekuwa afadhali afungiwe shingoni jiwe la kusagia[g] kama lile ambalo huzungushwa na punda na azamishwe katika bahari kuu.[h]

7 "Ole wake ulimwengu kwa sababu ya vikwazo! Bila shaka, vikwazo hivyo lazima vije,[i] lakini ole wake mtu ambaye kikwazo[j] huja kupitia kwake! **8** Basi, ikiwa mkono wako au mguu wako unakufanya ukwazike, ukate na kuutupa mbali nawe;[k] ni afadhali uingie katika uzima ukiwa kilema au ukiwa kiwete kuliko kutupwa ndani ya moto wa milele ukiwa na mikono miwili au miguu miwili.[l] **9** Pia, ikiwa jicho lako linakufanya ukwazike, ling'oe na kulitupa mbali nawe; ni afadhali uingie katika uzima ukiwa na jicho moja kuliko kutupwa katika Gehena* ya moto ukiwa na macho mawili.[m] **10** Angalieni msimdharau mmoja wa hawa wadogo; kwa maana ninawaambia ninyi

SURA 17
a Mt 21:21 Mk 11:23 Lu 17:6 1Ko 13:2
b 2Sa 24:14 Mt 20:18 Mk 9:31 Lu 9:44
c Mt 16:21 Mt 28:6
d Mk 9:32 Lu 9:45
e Kut 30:13 Kut 38:26
f Ro 14:13 1Ko 8:13 1Ko 10:32 2Ko 6:3
g Mk 12:17 Ro 13:7

SURA 18
h Mk 9:34 Lu 9:46 Lu 22:24

Safu ya 2
a Mk 9:36
b Mt 19:14 1Ko 14:20 1Pe 2:2
c Lu 18:17
d Mt 20:26 Mt 23:12 Lu 14:11 Lu 22:26 Yak 4:10
e Met 15:33 Lu 9:48 1Pe 5:5
f Mk 9:37
g Ufu 18:21
h Mk 9:42 Lu 17:2
i Mt 26:24
j Lu 17:1
k Mt 5:29 Mk 9:43 Kol 3:5
l Mt 25:41
m Mt 5:22 Mt 5:29 Mk 9:47 Ro 8:13

Mt 18:9* Bonde la Hinomu. Tazama Nyongeza 2.

kwamba malaika zao[a] mbinguni sikuzote huuona uso wa
Baba yangu aliye mbinguni.[b]
11 ——
12 "Mnaonaje? Mtu akiwa
na kondoo 100 na mmoja apotee,[c] je, hatawaacha wale 99
milimani na kuondoka kwenda kumtafuta yule anayepotea?[d] **13** Naye akimpata, hakika ninawaambia ninyi, yeye
humshangilia huyo zaidi kuliko wale 99 ambao hawakupotea.[e] **14** Vivyo hivyo Baba
yangu aliye mbinguni hatamani kwamba mmoja wa wadogo
hawa aangamie.[f]
15 "Zaidi ya hayo, ndugu
yako akitenda dhambi, nenda ufunue kosa lake kati yako
na yeye peke yake.[g] Akikusikiliza, umempata ndugu yako.[h]
16 Lakini asiposikiliza, chukua pamoja nawe mmoja au
wawili zaidi, ili kwa kinywa cha mashahidi wawili au watatu kila jambo lipate kuthibitishwa.[i] **17** Asipowasikiliza hao, liambie kutaniko. Ikiwa halisikilizi hata kutaniko, mwache awe kwako kama mtu
wa mataifa[j] na kama mkusanya-kodi.[k]
18 "Kwa kweli ninawaambia
ninyi, Mambo yoyote mtakayofunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni, na mambo
yoyote mtakayofungua duniani yatakuwa yamefunguliwa
mbinguni.[l] **19** Tena kwa kweli ninawaambia ninyi, Wawili
kati yenu wakikubaliana duniani kuhusu jambo lolote lenye
maana ambalo wanapaswa kuomba, litatendeka kwao kwa
sababu ya Baba yangu aliye mbinguni.[m] **20** Kwa maana pali-
po na wawili au watatu wakiwa
wamekusanyika pamoja katika
jina langu,[a] hapo mimi nipo katikati yao."[b]
21 Ndipo Petro akaja na
kumwambia: "Bwana, ndugu yangu atanitendea dhambi
mara ngapi nami nimsamehe?[c] Mpaka mara 7?"[d]
22 Yesu akamwambia: "Ninakuambia, si, Mpaka mara 7,
bali, Mpaka mara 77.[e]
23 "Ndiyo sababu ufalme wa
mbinguni umekuwa kama mtu,
mfalme,[f] aliyetaka kufanya hesabu[g] pamoja na watumwa
wake. **24** Alipoanza kuzifanya, mtu ambaye alikuwa na
deni lake la talanta elfu kumi [=dinari 60,000,000] akaletwa. **25** Lakini kwa sababu hakuwa na uwezo wa kulipa, bwana wake akaagiza yeye
na mke wake na watoto wake
na vitu vyote alivyokuwa navyo wauzwe na malipo yatolewe.[h] **26** Ndipo mtumwa huyo
akaanguka chini na kuanza kumsujudia, akisema, 'Uwe na subira kwangu nami nitakulipa
kila kitu.' **27** Akisikitishwa
na hayo, bwana wa mtumwa
huyo akamwachilia[i] na kufuta deni lake.[j] **28** Lakini mtumwa huyo akatoka, akamkuta mmoja wa watumwa wenzake aliyekuwa na deni lake la dinari[k] mia moja; akamkamata,
akamkaba koo, akisema, 'Lipa
deni lako lote.' **29** Basi mtumwa mwenzake akaanguka chini na kuanza kumsihi, akisema, 'Uwe na subira[l] kwangu
nami nitakulipa.' **30** Hata hivyo, yeye hakutaka, bali akaenda zake na kufanya atupwe
gerezani mpaka alipe deni
lake. **31** Kwa hiyo, watumwa

SURA 18
a Mdo 12:15
Ebr 1:14
b Lu 1:19
c 1Pe 2:25
d Lu 15:4
e Lu 15:6
f Lu 15:7
2Pe 3:9
g Law 19:17
Met 25:9
Lu 17:3
h Yak 5:20
i Kum 19:15
Yoh 8:17
2Ko 13:1
1Ti 5:19
Ebr 10:28
j Yoh 18:28
Mdo 10:28
Mdo 11:3
k Ro 16:17
1Ko 5:11
l Mt 16:19
Yoh 20:23
m Mk 11:24
Yoh 14:13
Yoh 16:24
1Yo 3:22
1Yo 5:14

Safu ya 2
a 1Ko 5:4
b Mt 28:20
c Met 19:11
d Mt 6:12
e Mk 11:25
Lu 17:4
Efe 4:32
Kol 3:13
f Mt 22:2
g Ro 14:12
h Kut 21:7
Law 25:39
2Fa 4:1
Ne 5:8
i Lu 7:42
j 1Yo 1:9
k Lu 7:41
l Mt 18:26

wenzake walipoona mambo
yaliyokuwa yametendeka, wa-
kahuzunika sana, nao wakaa-
nda na kumweleza bwana wao
mambo yote yaliyokuwa ya-
metendeka.[a] **32** Ndipo bwa-
na wake akamwita na kumwa-
mbia, 'Mtumwa mwovu, nilifu-
ta lile deni lote kwa ajili yako,
uliponisihi. **33** Haikukupasa
wewe, nawe, kuwa na rehe-
ma[b] juu ya mtumwa mwenzako,
kama mimi pia nilivyokuwa na
rehema[c] juu yako?' **34** Ndipo
bwana wake, akiwa na ghadha-
bu,[d] akamtia mikononi mwa
walinzi wa jela, mpaka alipe
deni lake lote. **35** Vivyo hi-
yo[e] Baba yangu wa mbinguni
atashughulika nanyi pia ikiwa
kila mmoja wenu hatamsame-
he ndugu yake kutoka moyoni
mwake."[f]

19 Basi Yesu alipokuwa ame-
maliza maneno hayo, aka-
ondoka Galilaya na kuja kwe-
nye mipaka ya Yudea ng'a-
mbo ya Yordani.[g] **2** Pia, uma-
ti mkubwa ukamfuata, naye
akawaponya huko.[h]

3 Na Mafarisayo wakamjia,
wakikusudia kumjaribu na ku-
sema: "Je, ni halali mwana-
mume kumtaliki mke wake
kwa kila sababu?"[i] **4** Akajibu,
akasema: "Je, hamkusoma kwa-
mba yeye aliyewaumba hao ku-
toka mwanzo aliwafanya mwa-
namume na mwanamke[j] **5** na
kusema, 'Kwa sababu hiyo
mwanamume atamwacha baba
yake na mama yake[k] naye ata-
shikamana na mke wake, na
hao wawili watakuwa mwili
mmoja'?[l] **6** Hivi kwamba wao
si wawili tena, bali mwili mmo-
ja. Kwa hiyo, kile ambacho Mu-

SURA 18
a Law 5:1
b Mt 6:12
Mt 7:12
Yak 2:13
c Isa 55:7
d Mt 22:7
e Ayu 34:11
Zb 62:12
Met 24:12
Ro 2:6
f Met 21:13
Mt 6:14
Mk 11:25
Lu 17:3
Efe 4:32

SURA 19
g Mk 10:1
Yoh 10:40
h Mt 12:15
Mt 14:14
Mt 15:30
Lu 5:15
i Kum 24:1
Mt 16:1
Mk 10:2
j Mwa 1:27
Mwa 5:2
Mk 10:6
k Mk 10:7
Efe 5:31
l Mwa 2:24

Safu ya 2
a Mk 10:9
1Ko 7:11
b Kum 24:1
Mt 5:31
c Mk 10:5
d Mwa 2:24
e Mal 2:14
Mt 5:32
Mk 10:11
Lu 16:18
Ro 7:3
1Ko 7:10
Ebr 13:4
f 1Ko 7:8
1Ko 7:38
1Ko 7:40
g 1Ko 7:7
h Kum 23:1
Isa 56:3
i 1Ko 7:32
1Ko 7:38
1Ko 9:5
j Mk 10:13
Lu 18:15
k Mt 18:3
Mk 10:14
Lu 18:16
l Mk 10:16

ngu ameunganisha mtu yeyo-
te asikitenganishe."[a] **7** Waka-
mwambia: "Basi, kwa nini Musa
aliagiza kutoa cheti cha kufu-
kuza na kumtaliki?"[b] **8** Aka-
waambia: "Musa, kwa kufiki-
ria ugumu wenu wa moyo,[c]
aliwapa ruhusa ya kuwatali-
ki wake zenu, lakini haikuwa
hivyo kutoka mwanzo.[d] **9** Ni-
nawaambia kwamba mtu yeyo-
te anayemtaliki mke wake na
kumwoa mwingine, ila kwa sa-
babu ya uasherati, anafanya
uzinzi."[e]

10 Wanafunzi wakamwa-
mbia: "Ikiwa hivyo ndivyo ili-
vyo kati ya mwanamume na
mke wake, ni afadhali kuto-
oa."[f] **11** Akawaambia: "Si
watu wote wanaolipa nafa-
si neno hilo, ila tu wale walio
na hiyo zawadi.[g] **12** Kwa ma-
ana kuna matowashi waliozali-
wa namna hiyo kutoka katika
tumbo la uzazi la mama yao,[h]
na kuna matowashi waliofa-
nywa matowashi na watu, na
kuna matowashi ambao wame-
jifanya wenyewe matowashi
kwa sababu ya ufalme wa mbi-
nguni. Yule anayeweza kulipa
nafasi na alipe nafasi."[i]

13 Ndipo akaletewa watoto
wachanga, ili aweke mikono
yake juu yao na kutoa sala; la-
kini wanafunzi wakawakemea.[j]
14 Hata hivyo, Yesu akasema:
"Waacheni watoto wachanga,
na acheni kuwazuia wasini-
jie, kwa maana ufalme wa mbi-
nguni ni wa watu walio kama
wao."[k] **15** Naye akaweka mi-
kono yake juu yao, akaondoka
hapo.[l]

16 Sasa, tazama! mtu fulani
akamjia na kusema: "Mwalimu,

nifanye wema gani ili niupate
uzima wa milele?"[a] **17** Aka-
mwambia: "Kwa nini unaniuli-
za juu ya lililo jema?[b] Kuna
mmoja tu aliye mwema. Inga-
wa hivyo, ikiwa unataka kui-
ngia katika uzima, zishike amri
sikuzote."[c] **18** Akamwambia:
"Amri gani?"[d] Yesu akasema:
"Naam, Usiue,[e] Usifanye uzi-
nzi,[f] Usiibe,[g] Usitoe ushahidi
wa uwongo,[h] **19** Mheshimu
baba yako na mama yako,[i] na,
Mpende jirani yako kama wewe
mwenyewe."[j] **20** Huyo kija-
na akamwambia: "Nimeyashi-
ka yote hayo; ni nini bado nina-
chokosa?" **21** Yesu akamwa-
mbia: "Ikiwa unataka kuwa
mkamilifu, nenda ukauze mali
zako na uwape maskini nawe
utakuwa na hazina mbingu-
ni,[k] kisha uje uwe mfuasi wa-
ngu."[l] **22** Huyo kijana alipo-
sikia maneno hayo, akaenda
zake akiwa amehuzunika, kwa
maana alikuwa na mali nyi-
ngi.[m] **23** Lakini Yesu akawa-
ambia wanafunzi wake: "Kwa
kweli ninawaambia ninyi kwa-
mba itakuwa vigumu kwa taji-
ri kuingia katika ufalme wa
mbinguni.[n] **24** Tena ninawa-
ambia ninyi, Ni rahisi zaidi
ngamia kupita katika tundu la
sindano kuliko tajiri kuingia
katika ufalme wa Mungu."[o]
25 Wanafunzi waliposikia
hilo, wakashangaa sana, wa-
kisema: "Ni nani kwa kwe-
li anayeweza kuokolewa?"[p]
26 Akiwatazama usoni, Yesu
akawaambia: "Kwa wanadamu
jambo hilo haliwezekani, la-
kini kwa Mungu mambo yote
yanawezekana."[q]
27 Ndipo Petro akamjibu na
kumwambia: "Tazama! Tume-
acha vitu vyote na kukufu-
ata wewe; kwa kweli kutaku-
wa na nini kwa ajili yetu?"[a]
28 Yesu akawaambia: "Kwa
kweli ninawaambia ninyi, Ka-
tika uumbaji-mpya Mwana
wa binadamu atakapoketi juu
ya kiti chake cha ufalme
chenye utukufu, ninyi ambao
mmenifuata mtaketi pia juu ya
viti vya ufalme kumi na viwi-
li, mkiyahukumu yale maka-
bila kumi na mawili ya Isra-
eli.[b] **29** Na kila mtu ambaye
ameacha nyumba au ndugu au
dada au baba au mama au wa-
toto au mashamba kwa ajili ya
jina langu atapokea mara nyi-
ngi zaidi naye atarithi uzima
wa milele.[c]
30 "Lakini wengi walio wa
kwanza watakuwa wa mwisho
na wa mwisho watakuwa wa
kwanza.[d]

20 "Kwa maana ufalme wa
mbinguni ni kama mtu,
mwenye nyumba, aliyetoka
asubuhi na mapema kwenda
kuajiri wafanyakazi kwa aji-
li ya shamba lake la mizabi-
bu.[e] **2** Alipokuwa amekubali-
ana na wafanyakazi hao awa-
lipe dinari moja kwa siku,[f] aka-
watuma katika shamba lake
la mizabibu. **3** Akatoka pia
karibu saa tatu,[g] akaona wengi-
ne wasio na kazi wakiwa wa-
mesimama sokoni;[h] **4** akawa-
ambia hao, 'Ninyi pia, nende-
ni katika shamba la mizabibu,
nami nitawapa kilicho haki.'
5 Kwa hiyo wakaenda. Tena
akatoka karibu saa sita[i] na
saa tisa[j] na kufanya vivyo hi-
vyo. **6** Mwishowe, karibu saa
kumi na moja akatoka, aka-
kuta wengine wakiwa wamesi-

SURA 19
a Mt 19:29 Mk 10:17 Lu 10:25 Lu 18:18
b Mk 10:18
c Law 18:5 Lu 10:28 Lu 18:20
d Lu 10:26
e Kut 20:13 Kum 5:17 Ro 13:9
f Kut 20:14 Kum 5:18
g Kut 20:15 Kum 5:19
h Kut 20:16 Kum 5:20
i Kut 20:12 Kum 5:16
j Law 19:18 Mt 22:39 Mk 12:31 Lu 10:27
k Mt 6:20
l Lu 12:33 Lu 18:22 Flp 3:7
m Zb 62:10 Mk 10:22 Lu 18:23
n Mk 10:23 Lu 18:24 1Ti 6:10
o Mk 10:25 Lu 18:25
p Mk 10:26
q Mwa 18:14 Ayu 42:2 Yer 32:17 Zek 8:6 Lu 18:27

Safu ya 2
a Mk 10:28 Lu 5:11 Lu 18:28 Flp 3:8
b Da 7:14 Mt 20:21 Mt 25:31 Lu 18:29 Lu 22:30 1Ko 6:2 Ufu 20:4
c Mk 10:30 Lu 18:29 Lu 18:30 Ebr 10:34
d Mt 20:16 Mk 10:31 Lu 13:30

SURA 20
e Isa 5:1 Mt 21:33
f Ufu 6:6
g Mk 15:25 Mdo 2:15
h Mdo 17:17
i Mk 15:33 Yoh 4:6
j Mt 27:45

mama, naye akawaambia, 'Kwa
nini mmekuwa mkisimama
hapa mchana wote bila kazi?'
7 Wakamwambia, 'Kwa saba-
bu hakuna mtu ambaye ameta-
ajiri.' Akawaambia, 'Ninyi pia
nendeni katika shamba la mi-
zabibu.'[a]

8 "Ilipofika jioni,[b] bwana wa
shamba la mizabibu akamwa-
mbia msimamizi wake, 'Waite
wafanyakazi na kuwalipa
mshahara wao,[c] ukianza na
yule wa mwisho mpaka yule
wa kwanza.' **9** Wale watu wa
saa kumi na moja walipokuja,
wakapokea kila mmoja dinari
moja. **10** Kwa hiyo, wale wa
kwanza walipokuja, wakakata
kauli kwamba wangepokea zai-
di; lakini wao pia wakalipwa
dinari moja. **11** Walipoipo-
kea wakaanza kumnung'unikia
mwenye nyumba[d] **12** na ku-
sema, 'Hawa wa mwisho walifa-
nya kazi kwa saa moja; na bado
umewafanya kuwa sawa na sisi
tuliofanya kazi ngumu mchana
kutwa katika lile joto lenye ku-
choma!' **13** Lakini akamjibu
mmoja wao, akasema, 'Mwe-
nzangu, sikutendei kosa. Tuli-
kubaliana dinari moja, sivyo?[e]
14 Chukua kilicho chako ue-
nde. Ninataka kumpa huyu wa
mwisho sawasawa na wewe.[f]
15 Je, si halali kwangu kufa-
nya kile ninachotaka na vitu
vyangu mwenyewe? Au jicho
lako ni ovu[g] kwa sababu mimi
ni mwema?'[h] **16** Vivyo hivyo
walio wa mwisho watakuwa
wa kwanza, na walio wa kwa-
nza watakuwa wa mwisho."[i]

17 Alipokuwa akikaribia
kupanda kwenda Yerusalemu,
Yesu akawapeleka wale wana-
funzi kumi na wawili[j] faragha-
ni na kuwaambia wakiwa ba-
rabarani: **18** "Tazameni! Tu-
napanda kwenda Yerusalemu,
na Mwana wa binadamu atati-
wa mikononi mwa wakuu wa
makuhani na waandishi, nao
watamhukumia kifo,[a] **19** na
watamtia mikononi mwa watu
wa mataifa wamdhihaki na ku-
mpiga mijeledi na kumtundi-
ka[b] juu ya mti, na siku ya tatu
atafufuliwa."[c]

20 Ndipo mama ya wana wa
Zebedayo[d] akamkaribia akiwa
pamoja na wanawe, akamsuju-
dia na kuomba kitu fulani ku-
toka kwake.[e] **21** Akamuuli-
za: "Unataka nini?" Akamji-
bu: "Toa agizo ili hawa wa-
nangu wawili waketi, mmoja
upande wako wa kuume na
mmoja upande wako wa ku-
shoto, katika ufalme wako."[f]
22 Yesu akamjibu, akasema:
"Hamjui kile mnachoomba.
Je, mnaweza kunywa kiko-
mbe[g] ambacho niko karibu ku-
nywa?" Wakamwambia: "Tu-
naweza." **23** Akawaambia:
"Kwa kweli mtakunywa ki-
kombe changu,[h] lakini kuke-
ti upande wangu wa kuume
na upande wangu wa kusho-
to sina haki ya kutoa, bali wa-
taketi wale ambao Baba yangu
amewatayarishia."[i]

24 Wale wengine kumi wa-
liposikia jambo hilo, wakawa-
ghadhibikia hao ndugu wawi-
li.[j] **25** Lakini Yesu akawaita,
akasema: "Mnajua kwamba
watawala wa mataifa hupi-
ga ubwana juu yao na wakuu
hutumia mamlaka juu yao.[k]
26 Hivyo sivyo ilivyo katika-
ti yenu;[l] bali yeyote anayeta-
ka kuwa mkubwa katikati yenu

SURA 20
a Yoh 15:8
b Amu 19:16
c Law 19:13
Kum 24:15
d Mt 13:27
e Mt 20:2
f Yoh 17:2
g Kum 15:9
Mt 6:23
Mk 7:22
h 1Pe 2:3
i Mt 19:30
Mk 9:35
Mk 10:31
Lu 13:30
j Mk 10:32
Lu 18:31

Safu ya 2
a Mt 16:21
Lu 9:22
b Mt 27:31
Yoh 19:1
c Mt 17:23
Mt 28:6
Mk 10:34
Lu 18:33
Mdo 10:40
1Ko 15:4
d Mt 4:21
Mt 27:56
e Mk 10:35
f Mt 19:28
Mk 10:37
g Mt 26:39
Mk 14:36
Yoh 18:11
h Mdo 12:2
Ro 8:17
2Ko 1:7
Ufu 1:9
i Mk 10:40
j Mk 10:41
Lu 22:24
k 1Ko 2:6
2Ko 1:24
l 1Pe 5:3

lazima awe mhudumu wenu,[a]
27 na yeyote anayetaka kuwa
wa kwanza katikati yenu la-
zima awe mtumwa wenu.[b]
28 Kama vile Mwana wa bina-
damu alivyokuja, si kuhudumi-
wa, bali kuhudumu[c] na kutoa
nafsi yake kuwa fidia badala ya
wengi."[d]

29 Sasa walipokuwa wakie-
nda kutoka Yeriko[e] umati mku-
bwa ukamfuata. **30** Na, ta-
zama! wanaume wawili vipofu
walikuwa wameketi kando ya
barabara, waliposikia kwamba
Yesu anapitia hapo, wakapaaza
sauti, wakisema: "Bwana, utu-
rehemu, Mwana wa Daudi!"[f]
31 Lakini umati ukasisitiza
kuwaambia wakae kimya; na
bado wakapaaza sauti kubwa
hata zaidi, wakisema: "Bwana,
uturehemu, Mwana wa Dau-
di!"[g] **32** Kwa hiyo Yesu aka-
simama, akawaita na kusema:
"Mnataka niwatendee nini?"
33 Wakamwambia: "Bwana,
tunataka macho yetu yafungu-
liwe."[h] **34** Yesu akawasikiti-
kia, akayagusa macho yao,[i] na
mara moja wakapata kuona,
nao wakamfuata.[j]

21 Basi, walipokaribia Ye-
rusalemu na kufika
Bethfage katika Mlima wa Mi-
zeituni, Yesu akawatuma wa-
wili kati ya wanafunzi wake,[k]
2 akawaambia: "Shikeni njia
mkaingie katika kijiji mnacho-
kiona mbele yenu, nanyi mara
moja mtakuta punda amefu-
ngwa, na mwana-punda pamo-
ja naye; wafungueni na kuwa-
leta kwangu.[l] **3** Na mtu aki-
waambia jambo lolote, seme-
ni, 'Bwana anawahitaji.' Ndipo
atawaacha mara moja."

SURA 20
a Mt 18:4
Mt 23:11
Mk 10:43
Lu 22:26
b Mk 9:35
Mk 10:44
c Lu 22:27
Yoh 13:14
Flp 2:7
d Law 4:21
Isa 53:11
1Ti 2:6
Tit 2:14
Ebr 9:28
e Mk 10:46
Lu 18:35
f Mt 9:27
Mt 15:22
Mk 10:47
Lu 18:38
g Lu 18:39
h Lu 18:41
i Mt 9:29
j Mk 10:52
Lu 18:43

SURA 21
k Mk 11:1
Lu 19:29
l Mk 11:2
Lu 19:30

Safu ya 2
a Isa 62:11
Yoh 12:15
b Mt 11:29
c Zek 9:9
d 1Fa 1:38
Lu 19:35
Yoh 12:14
e 2Fa 9:13
Lu 19:36
f 1Fa 1:40
Yoh 12:13
g Zb 118:25
Mt 9:27
Mt 21:15
h Zb 118:26
Mt 23:39
Lu 13:35
Yoh 5:43
Yoh 12:13
i Lu 2:14
j Mk 11:11
k Mt 21:46
Lu 7:16
Lu 24:19
l Mk 11:15
Lu 19:45
Yoh 2:15

4 Kwa kweli hilo lilitukia ili
litimizwe lililosemwa kupi-
tia nabii, akisema: **5** "Mwa-
mbieni binti Sayuni, 'Taza-
ma! Mfalme wako anakuja kwa-
ko,[a] mwenye tabia-pole,[b] naye
amepanda juu ya punda, ndiyo,
juu ya mwana-punda, uzao wa
mnyama wa kubeba mizigo.'"[c]

6 Kwa hiyo wanafunzi wa-
kaondoka, wakaenda na kufa-
nya kama vile Yesu alivyowaa-
giza. **7** Nao wakamleta huyo
punda na mwana-punda wake,
nao wakaweka juu yao mava-
zi yao ya nje, naye akaketi juu
yake.[d] **8** Walio wengi katika
umati wakatandaza mavazi[e]
yao ya nje barabarani, nao we-
ngine wakaanza kukata mata-
wi kutoka kwenye miti na ku-
yatandaza barabarani.[f] **9** Na
ule umati, wale waliokuwa wa-
kienda mbele yake na wale
waliokuwa wakifuata wakawa
wakipaaza sauti: "Mwokoe
Mwana wa Daudi, tunaomba![g]
Aliyebarikiwa ni yule anaye-
kuja katika jina la Yehova![h]
Mwokoe, tunaomba, katika vi-
lele vilivyo juu!"[i]

10 Basi alipoingia Yerusalem,[j] jiji lote likawa na msu-
kosuko, na kusema: "Ni nani
huyu?" **11** Umati ukawa uki-
sema: "Huyu ndiye nabii[k] Yesu,
kutoka Nazareti ya Galilaya!"

12 Na Yesu akaingia katika
hekalu na kuwafukuza wale
wote waliokuwa wakiuza na
kununua katika hekalu, na ku-
zipindua meza za wale wali-
kuwa wakibadili pesa na
viti vya wale waliokuwa waki-
uza njiwa.[l] **13** Naye aka-
waambia: "Imeandikwa, 'Nyu-
mba yangu itaitwa nyumba

ya sala,'[a] lakini ninyi mnaifanya kuwa pango la wanyang'anyi."[b] **14** Pia, vipofu na vilema wakamwendea hekaluni, naye akawaponya.

15 Wakuu wa makuhani na waandishi walipoyaona mambo ya kustaajabisha aliyofanya[c] na wale wavulana waliokuwa wakipaaza sauti katika hekalu na kusema: "Mwokoe Mwana wa Daudi, tunaomba!"[d] wakaghadhibika **16** na kumwambia: "Je, unasikia mambo ambayo hawa wanasema?" Yesu akawaambia: "Ndiyo. Je, ninyi hamkusoma hili kamwe,[e] 'Kutoka katika kinywa cha watoto na wanaonyonya umetoa sifa'?"[f] **17** Naye akawaacha, akaenda nje ya jiji mpaka Bethania na kukaa huko usiku.[g]

18 Alipokuwa akirudi jijini asubuhi na mapema, aliona njaa.[h] **19** Naye akaona mtini kando ya barabara na kuendea, lakini hakukuta kitu[i] juu yake ila majani tu, naye akauambia: "Usizae matunda yoyote tena kamwe, milele."[j] Nao mtini ukanyauka mara moja. **20** Lakini wanafunzi walipoona hilo, wakastaajabu, wakasema: "Imewezekanaje mtini ukanyauka mara moja?"[k] **21** Yesu akajibu, akawaambia: "Kwa kweli ninawaambia ninyi, Ikiwa tu mna imani nanyi msitie shaka,[l] hamtafanya nililofanya kwa mtini huo tu, bali pia mkiuambia mlima huu, 'Ondoka, ukatupwe baharini,' jambo hilo litatukia.[m] **22** Na mambo yote mnayoomba katika sala, mkiwa na imani, mtapokea."[n]

23 Basi alipoingia ndani ya hekalu, wakuu wa makuhani na wanaume wazee wa watu wakamjia alipokuwa akifundisha, nao wakasema:[a] "Unafanya mambo haya kwa mamlaka gani? Na ni nani aliyekupa mamlaka hiyo?"[b] **24** Yesu akajibu, akawaambia: "Mimi pia, nitawauliza ninyi jambo moja. Mkiniambia jambo hilo, mimi pia nitawaambia ninyi ninafanya mambo haya kwa mamlaka gani:[c] **25** Ule ubatizo wa Yohana, ulitoka wapi? Mbinguni au kwa wanadamu?"[d] Lakini wakaanza kujadiliana kati yao wenyewe, wakisema: "Tukisema, 'Ulitoka mbinguni,' atatuambia, 'Basi, kwa nini hamkumwamini?'[e] **26** Hata hivyo, tukisema, 'Ulitoka kwa wanadamu,' tunaogopa umati,[f] kwa maana wao wote wanamwona Yohana kuwa nabii."[g] **27** Kwa hiyo wakamjibu Yesu, wakasema: "Hatujui." Yeye naye akawaambia: "Wala mimi siwaambii ninyi ninafanya mambo haya kwa mamlaka gani.[h]

28 "Mnaonaje? Mtu alikuwa na watoto wawili.[i] Akamwendea wa kwanza, akasema, 'Mwanangu, leo nenda ukafanye kazi katika shamba la mizabibu.' **29** Akajibu, akasema, 'Nitaenda,[j] bwana,' lakini hakuenda. **30** Akamwendea yule wa pili, akasema jambo hilohilo. Naye akamjibu, akasema, 'Sitaenda.' Baadaye akajuta,[k] akaenda. **31** Ni yupi kati ya hao wawili aliyefanya mapenzi ya baba yake?"[l] Wakasema: "Huyo wa pili." Yesu akawaambia: "Kwa kweli ninawaambia kwamba wakusanya-kodi na makahaba wanawatangulia ninyi kuingia katika ufalme

SURA 21

a 2Nya 6:33
Isa 56:7
b Yer 7:11
Mk 11:17
Lu 19:46
Yoh 2:16
c Mk 11:18
d Zb 118:25
Mt 21:9
e Lu 6:3
f Zb 8:2
g Mk 11:11
Lu 21:37
Yoh 11:1
h Mk 11:12
i Mk 11:13
Lu 13:6
j Mt 3:10
k Mk 11:21
l Yak 1:6
m Mt 17:20
Lu 17:6
1Ko 13:2
n Mk 11:24
Lu 11:9
Yoh 14:13
Yak 1:5
1Yo 3:22

Safu ya 2

a Mk 11:27
Lu 20:1
b Kut 2:14
Lu 20:2
Yoh 2:18
Mdo 4:7
c Mk 11:29
d Lu 20:4
Yoh 1:33
e Mt 21:32
Mk 11:31
Lu 7:30
f Mt 14:5
Mt 21:46
g Mk 11:32
Lu 20:6
h Lu 20:8
i Lu 15:11
j Mt 7:21
Lu 6:46
k Met 24:32
l Lu 18:14

wa Mungu. **32** Kwa maana
Yohana alikuja kwenu katika
njia ya uadilifu,[a] lakini hamku-
mwamini.[b] Hata hivyo, waku-
sanya-kodi na makahaba wa-
limwamini,[c] nanyi, ijapokuwa
mliona hilo, hamkujuta baada-
ye ili kumwamini.
33 "Sikilizeni mfano mwi-
ngine: Kulikuwa na mtu, mwe-
nye nyumba,[d] aliyepanda sha-
mba la mizabibu, akaweka ua
kulizunguka, akachimba shi-
nikizo la divai ndani yake, aka-
simamisha mnara,[e] akaliko-
disha kwa wakulima, ki-
sha akasafiri kwenda ng'ambo.[f]
34 Majira ya matunda yalipo-
fika, akawatuma watumwa
wake kwa wakulima wakapa-
te matunda yake. **35** Hata hi-
vyo, wakulima wakawachu-
kua watumwa wake, waka-
mpiga mmoja sana, mwingine
wakamuua, mwingine waka-
mpiga kwa mawe.[g] **36** Tena
akawatuma watumwa wengi-
ne, zaidi ya wale wa kwanza,
lakini wakawatendea vivyo hi-
vyo.[h] **37** Mwishowe akamtu-
ma mwana wake kwao, aki-
sema, 'Watamheshimu mwa-
nangu.' **38** Walipomwona
mwana wakulima wakasame-
zana, 'Huyu ndiye mrithi;[i] njo-
oni, acheni tumuue na kuu-
pata urithi wake!'[j] **39** Kwa
hiyo wakamchukua na kumtu-
pa nje ya shamba la mizabibu
na kumuua.[k] **40** Basi, mwe-
nye shamba la mizabibu ataka-
pokuja, atawatendea nini wa-
kulima hao?" **41** Wakamwa-
mbia: "Kwa sababu wao ni wao-
vu, atawaharibu[l] hao vibaya
na kulikodisha shamba la mi-
zabibu kwa wakulima wengine,

SURA 21
a Mt 21:25
Lu 7:30
b Yoh 7:48
c Mk 2:15
Lu 3:12
Lu 7:29
d Mt 20:1
e Isa 5:2
Yer 2:21
f Mk 12:1
Lu 20:9
g Ne 9:26
Mt 22:6
Lu 20:10
h 2Nya 36:15
Mk 12:5
Mdo 7:52
1Th 2:15
Ebr 11:37
i Ebr 1:2
j Lu 20:14
k Mt 27:18
Mk 12:8
Mdo 2:23
Mdo 3:15
Ebr 13:12
l Zek 12:2

Safu ya 2
a Mk 12:9
Lu 20:16
Mdo 18:6
b Zb 118:22
1Pe 2:7
c Isa 28:16
Mk 12:10
Lu 20:17
Mdo 4:11
Ro 9:33
Efe 2:20
d Mt 8:12
Mt 22:9
Ebr 8:9
e Isa 8:14
Da 2:34
Da 2:44
Lu 20:18
1Pe 2:8
f Lu 20:19
g Mt 21:11
Mk 12:12
Yoh 7:32
Yoh 7:40

SURA 22
h Lu 14:16
i Mwa 29:22
Mt 9:15
Ufu 19:9
j Yoh 13:20
k Lu 14:17
l Mt 21:36
m Amu 14:10
n Ufu 19:9

ambao watampa matunda kwa
wakati wake."[a]
42 Yesu akawaambia: "Je,
hamkusoma kamwe katika
Maandiko, 'Jiwe ambalo waje-
nzi walilikataa[b] ndilo limeku-
wa jiwe kuu la pembeni.[c] Lime-
tokana na Yehova, nalo ni la
kustaajabisha machoni petu'?
43 Ndiyo sababu ninawaambia
ninyi, Ufalme wa Mungu uta-
chukuliwa kutoka kwenu
na kupewa taifa lenye kuzaa
matunda yake.[d] **44** Pia, mtu
atakayeangukia jiwe hilo ata-
vunjika-vunjika. Na yeyote
ambaye litamwangukia, lita-
mponda-ponda."[e]
45 Basi wakuu wa makuha-
ni na Mafarisayo walipokuwa
wamesikia mifano yake, wa-
kajua kwamba alikuwa aki-
sema juu yao.[f] **46** Lakini, ija-
pokuwa walikuwa wakitafuta
kumkamata, waliogopa umati,
kwa sababu walimwona kuwa
nabii.[g]

22 Yesu akawajibu kwa ku-
waambia mifano tena,
akisema:[h] **2** "Ufalme wa mbi-
nguni umekuwa kama mtu, mfa-
lme, aliyefanya karamu ya
ndoa[i] kwa ajili ya mwana wake.
3 Naye akatuma watumwa wake
wawaite wale walioalikwa kwe-
nye karamu ya ndoa,[j] lakini ha-
wakutaka kuja.[k] **4** Tena aka-
watuma watumwa wengine,[l] aki-
sema, 'Waambieni wale walioa-
likwa: "Tazama! Nimetayarisha
chakula changu cha mchana,[m]
ng'ombe-dume wangu na wa-
nyama waliononeshwa wame-
chinjwa, na vitu vyote viko ta-
yari. Njooni kwenye karamu ya
ndoa."'[n] **5** Lakini wakaenda

zao bila kujali, mmoja kwenye
shamba lake mwenyewe, mwi-
ngine kwenye kazi yake ya bi-
ashara;[a] **6** lakini wale wengi-
ne wakawashika watumwa
wake, wakawatendea kwa dha-
rau na kuwaua.[b]
7 "Lakini mfalme akawa na
ghadhabu, akayatuma majeshi
yake na kuwaangamiza wau-
aji hao na kulichoma jiji lao.[c]
8 Ndipo akawaambia watu-
mwa wake, 'Karamu ya ndoa
kwa kweli iko tayari, lakini
wale walioalikwa hawaku-
stahili.[d] **9** Kwa hiyo nendeni
kwenye barabara zinazotoka
jijini, na mtu yeyote mtakaye-
mkuta mwalikeni kwenye ka-
ramu ya ndoa.'[e] **10** Basi wa-
tumwa hao wakaenda bara-
barani na kuwakusanya wote
waliowakuta, waovu na wema
pia;[f] na chumba cha sherehe za
arusi kikajaa watu wenye ku-
keti[g] mezani.
11 "Mfalme alipoingia ku-
wakagua wageni walioalikwa
akamwona hapo mtu ambaye
hakuwa amevaa vazi la ndoa.[h]
12 Kwa hiyo akamwambia,
'Mwenzangu, uliingiaje humu
bila kuvaa vazi la ndoa?'[i]
Akakosa la kusema. **13** Ndi-
po mfalme akawaambia watu-
mishi wake, 'Mfungeni mikono
na miguu na kumtupa gizani,
kule nje. Huko ndiko atalia na
kusaga meno yake.'[j]
14 "Kwa maana wanaoali-
kwa ni wengi, lakini wanao-
chaguliwa ni wachache."[k]
15 Ndipo Mafarisayo wakao-
ndoka, wakaenda na kushau-
riana pamoja kusudi wamtege
kwa maneno yake.[l] **16** Basi
wakawatuma wanafunzi wao
kwake, pamoja na wafuasi wa
chama cha Herode,[a] wakise-
ma: "Mwalimu, tunajua wewe
una ukweli nawe hufundisha
njia ya Mungu katika kweli, na
hujali mtu yeyote, kwa maana
wewe hutazami sura ya mtu.[b]
17 Kwa hiyo, tuambie, Unaona-
je? Je, ni halali kumlipa Kai-
sari kodi au hapana?"[c] **18** La-
kini Yesu, akiujua uovu wao,
akasema: "Kwa nini mnanija-
ribu, enyi wanafiki?[d] **19** Ni-
onyesheni sarafu ya kodi ya
kichwa." Wakamletea dinari.
20 Naye akawaambia: "Sana-
mu hii na mwandiko huu ni
za nani?"[e] **21** Wakasema: "Ni
za Kaisari." Ndipo akawaambia:
"Basi, mlipeni Kaisari vitu vya
Kaisari, lakini Mungu vitu vya
Mungu."[f] **22** Basi, waliposi-
kia hilo, wakastaajabu, waka-
mwacha na kwenda zao.[g]
23 Siku hiyo Masadukayo,
wale ambao husema hakuna ufu-
fuo, wakamjia na kumuuliza:[h]
24 "Mwalimu, Musa alisema,
'Mtu yeyote akifa bila kuwa
na watoto, ndugu yake amwoe
mke wake na kumwinulia ndugu
yake uzao.'[i] **25** Basi kulikuwa
na ndugu saba; naye wa kwanza
akaoa na kufa, na, kwa kuwa ha-
kuwa na uzao, akamwachia ndu-
gu yake mke wake.[j] **26** Ika-
wa vivyo hivyo pia kwa yule
wa pili na yule wa tatu, mpaka
wote saba.[k] **27** Mwishowe yule
mwanamke akafa. **28** Kwa
hiyo, katika ufufuo, atakuwa
mke wa nani kati ya hao saba?
Kwa maana alikuwa mke wao
wote."[l]
29 Yesu akawajibu, akawaa-
mbia: "Ninyi mnakosea, kwa
sababu hamjui Maandiko wala

SURA 22
a Lu 14:18
b Mt 21:35
Mt 23:37
1Th 2:15
c Da 9:26
Lu 19:27
d Mdo 13:46
e Mt 21:43
Lu 14:21
f Mt 13:47
g Mk 2:15
h Ufu 19:8
i Efe 4:24
j Zb 112:10
Mt 8:12
Mt 13:42
Mt 24:51
Mt 25:30
k Mt 7:14
Lu 13:23
l Mk 12:13
Lu 20:20

Safu ya 2
a Mk 3:6
Mk 12:13
b Lu 20:21
Yoh 3:2
c Mt 17:25
Lu 20:22
d Mk 12:15
e Mk 12:16
f Da 3:18
Mal 3:8
Mk 12:17
Lu 20:25
Lu 23:2
Ro 13:7
g Lu 20:26
h Mk 12:18
Lu 20:27
Mdo 4:2
Mdo 23:8
i Mwa 38:8
Kum 25:5
Ru 1:11
Ru 3:13
Mk 12:19
j Lu 20:29
k Mk 12:21
Lu 20:31
l Mk 12:23
Lu 20:33

nguvu za Mungu;[a] **30** kwa maana katika ufufuo wanaume
hawaoi wala wanawake hawaolewi,[b] bali wao ni kama mala-
ika mbinguni. **31** Kwa habari ya ufufuo wa wafu, je, ha-
mkusoma mliloambiwa na Mungu, akisema,[c] **32** 'Mimi ni
Mungu wa Abrahamu na Mungu wa Isaka na Mungu wa
Yakobo'?[d] Yeye ni Mungu, si wa wafu, bali wa walio hai."[e]
33 Waliposikia hilo, umati wa-
kastaajabishwa na mafundisho
yake.[f]

34 Baada ya Mafarisayo
kusikia kwamba alikuwa ame-
wanyamazisha kimya Masadu-
kayo, wakakusanyika pamoja
katika kikundi kimoja. **35** Na
mmoja wao, mwenye ujuzi
wa Sheria,[g] akauliza, akimja-
ribu: **36** "Mwalimu, amri iliyo
kuu katika ile Sheria ni gani?"[h]
37 Akamwambia: "'Lazima
umpende Yehova Mungu wako
kwa moyo wako wote na kwa
nafsi yako yote na kwa akili
yako yote.'[i] **38** Hii ndiyo amri
iliyo kuu na ya kwanza. **39** Ya
pili, kama hiyo, ni hii, 'Mpende
jirani yako kama wewe mwe-
nyewe.'[j] **40** Sheria yote na
Manabii hutegemea amri hizo
mbili."[k]

41 Na Mafarisayo walipoku-
wa wamekusanyika pamoja,
Yesu akawauliza:[l] **42** "Mna
maoni gani kuhusu Kristo? Ni
mwana wa nani?" Wakamwa-
mbia: "Wa Daudi."[m] **43** Aka-
waambia: "Basi, kwa nini Daudi
akiongozwa na roho[n] anamwi-
ta 'Bwana,' akisema, **44** 'Ye-
hova alimwambia Bwana wa-
ngu: "Keti kwenye mkono wa-
ngu wa kuume mpaka niwawe-
ke adui zako chini ya miguu
yako"'?[a] **45** Kwa hiyo, ikiwa
Daudi anamwita 'Bwana,' ina-
wezekanaje kwamba yeye ni
mwana wake?"[b] **46** Na haku-
na mtu aliyeweza kumjibu hata
neno moja, na tangu siku hiyo
na kuendelea hakuna mtu yeyo-
te aliyethubutu tena kumuuliza
swali.[c]

23 Ndipo Yesu akasema na
umati na wanafunzi wa-
ke,[d] akisema: **2** "Waandi-
shi[e] na Mafarisayo wameji-
ketisha katika kiti cha Musa.[f]
3 Kwa hiyo mambo yote wana-
yowaambia ninyi,[g] yafanyeni
na kuyashika, lakini msifanye
kulingana na matendo yao,[h]
kwa maana wao husema lakini
hawatendi. **4** Wao hufunga
mizigo mizito na kuiweka juu
ya mabega ya watu,[i] lakini wao
wenyewe hawataki kuisoge-
za kwa kidole chao.[j] **5** Kazi
zote wanazozifanya wao huzi-
fanya ili watazamwe na watu;[k]
kwa maana wanapanua vibwe-
ta[l] vyenye maandiko amba-
vyo wao huvaa kama ulinzi,
na kuongeza ukubwa wa pindo
zenye nyuzinyuzi[m] za mava-
zi yao. **6** Wao hupenda ma-
hali penye kuonekana zaidi[n]
kwenye milo ya jioni na viti
vya mbele katika masinago-
gi,[o] **7** na salamu[p] katika ma-
soko na kuitwa Rabi na
watu.[q] **8** Lakini ninyi, msii-
twe Rabi, kwa maana mwa-
limu[r] wenu ni mmoja, lakini
ninyi nyote ni ndugu. **9** Zaidi
ya hayo, msimwite mtu yeyo-
te baba yenu duniani, kwa ma-
ana Baba[s] yenu ni mmoja, Yule
wa mbinguni. **10** Wala msii-
twe 'viongozi,'[t] kwa maana Ki-
ongozi wenu ni mmoja, Kristo.

SURA 22
a Mk 12:24
b Lu 20:35
c Mk 12:26
d Kut 3:6
Mdo 3:13
Ebr 11:16
e Lu 20:37
Lu 20:38
Ro 4:17
f Mt 7:28
Mk 11:18
g Lu 10:25
h Mk 12:28
i Kum 6:5
Kum 10:12
Yos 22:5
Mk 12:30
Lu 10:27
j Law 19:18
Mk 12:31
Lu 10:27
Kol 3:14
Yak 2:8
1Pe 1:22
k Ro 13:10
Ga 5:14
l Mk 12:35
m Lu 20:41
Yoh 7:42
n 2Sa 23:2

Safu ya 2
a Zb 110:1
Mdo 2:34
1Ko 15:25
Ebr 1:13
Ebr 10:13
b Mk 12:37
c Mk 12:34
Lu 20:40

SURA 23
d Lu 20:45
e Mk 12:38
f Kut 18:13
g Mal 2:7
h Mal 2:8
i Mt 11:28
Mdo 15:10
j Lu 11:46
k Mt 6:1
l Kum 6:8
m Hes 15:38
Kum 22:12
n Mk 12:39
Lu 14:7
Lu 14:10
o Lu 11:43
p Lu 20:46
q Ayu 32:22
r Yoh 13:13
s Mt 6:9
t 1Pe 5:3

11 Lakini aliye mkubwa zaidi
katikati yenu lazima awe mhu-
dumu wenu.[a] **12** Yeyote yule
anayejiinua atanyenyekezwa,[b]
na yeyote yule anayejinyenye-
keza atainuliwa.[c]
13 "Ole wenu ninyi, waa-
ndishi na Mafarisayo, wanafi-
ki! kwa sababu mnawafungia[d]
watu ufalme wa mbinguni;
kwa maana ninyi[e] wenyewe
hamwingii, wala hamwaruhu-
su wale wanaoenda huko wa-
ingie. **14** ——
15 "Ole wenu ninyi, waandi-
shi na Mafarisayo, wanafiki![f]
kwa sababu mnasafiri katika
bahari na katika nchi kavu ili
kugeuza imani ya mtu mmo-
ja, na anapogeuka ninyi hu-
mfanya astahili Gehena* mara
mbili zaidi kuliko ninyi we-
nyewe.
16 "Ole wenu ninyi, viongo-
zi vipofu,[g] mnaosema, 'Mtu ye-
yote akiapa kwa hekalu, si
kitu; lakini mtu yeyote akiapa
kwa dhahabu ya hekalu, ata-
kuwa na wajibu.'[h] **17** Wapu-
mbavu na vipofu! Kwa kweli,
ni kipi kilicho kikubwa zaidi,
dhahabu au hekalu ambalo li-
meitakasa dhahabu?[i] **18** Pia,
'Mtu yeyote akiapa kwa ma-
dhabahu, si kitu; lakini mtu ye-
yote akiapa kwa zawadi iliyo
juu yake, atakuwa na wajibu.'
19 Vipofu! Kwa kweli, ni kipi
kilicho kikubwa zaidi, zawa-
di au madhabahu[j] ambayo hui-
takasa zawadi? **20** Kwa hiyo
yeye anayeapa kwa madhaba-
hu anaapa kwa hiyo na kwa
vitu vyote vilivyo juu yake;

Mt 23:15* Bonde la Hinomu. Tazama Nyongeza 2.

SURA 23
a Mt 20:26
Mk 9:35
Lu 22:26
b Met 16:18
Met 29:23
c Met 15:33
Mt 18:4
Lu 14:11
Ro 12:3
Efe 4:2
1Pe 5:5
d Mt 16:19
e Lu 11:52
f Mt 6:2
Mt 7:5
Lu 12:56
g Mt 15:14
Ro 2:19
h Mt 5:34
i Kut 30:29
j Kut 29:37

Safu ya 2
a 1Fa 8:13
Zb 11:4
Zb 26:8
Zb 132:14
b Mt 5:34
c Law 27:30
Lu 11:42
d Yer 22:15
Yoh 7:24
e Ho 6:6
Mik 6:8
Mt 9:13
Mt 12:7
f 1Ti 1:5
g Mt 15:14
h Law 11:42
i Law 11:4
j Mk 7:4
k Mk 12:40
l Yoh 9:40
m Lu 11:39
n Lu 12:56
o Kum 27:4
Lu 11:44
Mdo 23:3
p Lu 16:15
q Mt 6:2

21 naye anayeapa kwa heka-
lu anaapa kwa hilo na kwa
yeye anayekaa ndani yake;[a]
22 naye anayeapa kwa mbi-
ngu anaapa kwa kiti cha ufa-
lme cha Mungu[b] na kwa yeye
anayeketi juu yake.
23 "Ole wenu ninyi, waandi-
shi na Mafarisayo, wanafiki!
kwa sababu ninyi huitoa sehe-
mu ya kumi[c] ya mnanaa na
dili na bizari, lakini mmepuu-
za mambo mazito zaidi ya She-
ria, yaani, haki[d] na rehema[e] na
uaminifu.[f] Ilikuwa lazima ku-
yafanya mambo haya, na bado
kutopuuza yale mambo me-
ngine. **24** Viongozi vipofu,[g]
ambao humchuja mbu[h] lakini
hummeza ngamia![i]
25 "Ole wenu ninyi, waandi-
shi na Mafarisayo, wanafiki!
kwa sababu ninyi husafisha
upande wa nje wa kikombe[j] na
wa sahani, lakini upande wa
ndani vimejaa vitu vilivyopor-
wa[k] na mambo yenye kupita ki-
asi. **26** Farisayo kipofu,[l] kwa-
nza safisha upande wa nda-
ni wa kikombe[m] na wa sahani,
ili upande wake wa nje upate
kuwa safi pia.
27 "Ole wenu ninyi, waandi-
shi na Mafarisayo, wanafiki![n]
kwa sababu mnafanana na ma-
kaburi yaliyopakwa chokaa,[o]
ambayo kwa nje yanaoneka-
na kwa kweli kuwa mazuri la-
kini ndani yamejaa mifupa ya
wafu na kila namna ya ukosefu
wa usafi. **28** Katika njia hiyo
ninyi pia, kwa kweli, mnaone-
kana kwa nje kuwa waadilifu
kwa watu,[p] lakini ndani mme-
jaa unafiki na uasi-sheria.
29 "Ole wenu ninyi, waandi-
shi na Mafarisayo, wanafiki![q]

kwa sababu mnajenga maka-
buri ya manabii na kuyarembe-
sha makaburi ya waadilifu,[a]
30 nanyi mnasema, ‘Kama tu-
ngekuwa katika siku za maba-
bu zetu, hatungekuwa washi-
riki pamoja nao katika damu
ya manabii.’[b] **31** Kwa hiyo
mnatoa ushahidi juu yenu we-
nyewe kwamba ninyi ni wana
wa wale waliowaua manabii.[c]
32 Hivyo, basi, kijazeni kipi-
mo[d] cha mababu zenu.

33 “Nyoka, uzao wa nyoka-
vipiri,[e] mtaikimbiaje hukumu
ya Gehena?*[f] **34** Kwa saba-
bu hiyo, tazameni, ninatuma[g]
kwenu manabii na watu wenye
hekima na wafundishaji wa
watu wote.[h] Baadhi yao mta-
waua[i] na kuwatundika mti-
ni, na baadhi yao mtawapiga
mijeledi[j] katika masinagogi
yenu na kuwatesa jiji baada ya
jiji; **35** ili ije juu yenu damu
yote ya uadilifu iliyomwagwa
juu ya dunia,[k] tangu damu[l] ya
Abeli[m] mwadilifu mpaka damu
ya Zekaria mwana wa Bara-
kia, ambaye mlimuua katikati
ya patakatifu na madhabahu.[n]
36 Kwa kweli ninawaambia
ninyi, Mambo yote haya yata-
kipata kizazi hiki.[o]

37 “Yerusalemu, Yerusale-
mu, muuaji wa manabii[p] na
ambaye huwapiga kwa mawe[q]
wale waliotumwa kwake,[r]
—ni mara ngapi nilitaka ku-
wakusanya watoto wako, kama
vile kuku anavyokusanya vi-
faranga vyake chini ya maba-
wa yake![s] Lakini hamkutaka.[t]
38 Tazama! Nyumba yenu[u]
mmeachiwa hali ya ukiwa.[v]

Mt 23:33* Bonde la Hinomu. Tazama Nyongeza 2.

SURA 23
a Lu 11:47
b Lu 11:50
c Lu 11:48
Mdo 7:52
Ebr 11:37
d 1Th 2:16
e Mwa 3:15
Mt 3:7
Mt 12:34
Lu 3:7
f Mt 10:28
Mk 12:40
Lu 12:5
g Lu 11:49
h Mt 10:41
Mt 13:52
i Mdo 7:59
j Lu 21:12
Yoh 16:2
Mdo 5:40
2Ko 11:24
1Th 2:15
k Mt 27:25
l Lu 11:50
Lu 11:51
Ufu 18:24
m Mwa 4:10
Ebr 11:4
n 2Nya 24:22
o Kut 20:5
p Lu 13:34
q Ebr 11:37
r 2Nya 24:21
Yoh 8:59
1Th 2:15
s Zb 91:4
t Lu 19:14
u 1Fa 9:7
Yer 12:7
Yer 22:5
Mt 21:43
Lu 19:42
v Lu 21:20

Safu ya 2
a Zb 118:26
Mt 21:9

SURA 24
b Mk 13:1
Lu 21:5
c Yer 7:14
Yer 26:18
Mik 3:12
Mt 22:7
Lu 19:44
d Mt 24:27
Mt 24:37
Mt 24:39
e Mt 13:39
Mt 28:20
Mk 13:4
Lu 21:7
f Yer 14:14
Mk 13:5
Lu 21:8
Kol 2:8
2Th 2:3
g Mt 24:24
h Mk 13:7
Lu 21:9
i Hag 2:22
Mk 13:8
Ufu 6:4
j Lu 21:10
k Mdo 11:28
Ufu 6:6
l Mk 13:8
Lu 21:11
m Mt 10:17
Yoh 15:20
Mdo 11:19
Ufu 2:10

39 Kwa maana ninawaambia
ninyi, Hamtaniona kamwe ta-
ngu sasa mpaka mtakaposema,
‘Aliyebarikiwa ni yule anaye-
kuja katika jina la Yehova!’”[a]

24 Sasa Yesu akaondoka,
akashika njia kutoka he-
kaluni, lakini wanafunzi wake
wakamkaribia na kumwo-
nyesha majengo ya hekalu.[b]
2 Akajibu, akawaambia: “Je,
hamvioni vitu vyote hivi? Kwa
kweli ninawaambia ninyi, Ha-
kuna jiwe litakaloachwa hapa
juu ya jiwe nalo lisiangushwe
chini.”[c]

3 Alipokuwa ameketi juu ya
Mlima wa Mizeituni, wanafu-
nzi wakamkaribia faraghani,
wakisema: “Tuambie, Mambo
haya yatakuwa wakati gani, na
ni nini itakayokuwa ishara ya
kuwapo[d] kwako na ya umalizio
wa mfumo wa mambo?”[e]

4 Naye Yesu akajibu, akawa-
ambia: “Jihadharini mtu yeyo-
te asiwapotoshe;[f] **5** kwa ma-
ana wengi watakuja kwa msi-
ngi wa jina langu, wakisema,
‘Mimi ndiye Kristo,’ nao wa-
tawapotosha wengi.[g] **6** Mta-
sikia juu ya vita na habari za
vita; angalieni kwamba msio-
gope. Kwa maana mambo hayo
lazima yatukie, lakini ule mwi-
sho bado.[h]

7 “Kwa maana taifa litasi-
mama kupigana na taifa[i] na
ufalme kupigana na ufalme,[j]
kutakuwa na upungufu wa
chakula[k] na matetemeko ya
nchi[l] mahali pamoja baada ya
pengine. **8** Mambo yote hayo
ni mwanzo wa maumivu ya ta-
abu.

9 “Ndipo watu watakapowa-
tia ninyi katika dhiki[m] na ku-

waua[a] ninyi, nanyi mtachukiwa[b] na mataifa yote kwa sababu ya jina langu.[c] **10** Ndipo, pia, watu wengi watakwazika[d] na kusalitiana na kuchukiana.[e] **11** Na manabii wengi wa uwongo[f] watatokea na kuwapotosha wengi;[g] **12** na kwa sababu ya kuongezeka kwa uasisheria[h] upendo wa walio wengi zaidi utapoa.[i] **13** Lakini yule ambaye atavumilia[j] mpaka mwisho ndiye atakayeokolewa.[k] **14** Na hii habari njema[l] ya ufalme[m] itahubiriwa katika dunia yote inayokaliwa ili kuwa ushahidi kwa mataifa yote;[n] na ndipo ule mwisho[o] utakapokuja.

15 "Kwa hiyo, mtakapoona lile chukizo[p] linalosababisha ukiwa, kama vile lilivyosemwa kupitia nabii Danieli, likiwa limesimama katika mahali patakatifu,[q] (msomaji na atumie utambuzi,) **16** ndipo wale walio katika Yudea waanze kukimbilia[r] milimani. **17** Mtu aliye juu ya paa ya nyumba asishuke kuchukua mali kutoka katika nyumba yake; **18** na mtu aliye shambani asirudi nyumbani kuchukua vazi lake la nje. **19** Ole wao wanawake wenye mimba na wale wanaonyonyesha mtoto mchanga katika siku hizo![s] **20** Endeleeni kusali kwamba kukimbia kwenu kusiwe wakati wa majira ya baridi kali, wala siku ya sabato; **21** kwa maana ndipo kutakapokuwa na dhiki kuu[t] ya namna ambayo haijapata kutukia tangu mwanzo wa ulimwengu mpaka sasa,[u] hapana, wala haitatukia tena. **22** Kwa kweli, kama siku hizo hazingefupishwa, hakuna chochote chenye mwili ambacho kingeokolewa; lakini kwa sababu ya wale waliochaguliwa[a] siku hizo zitafupishwa.[b]

23 "Ndipo mtu yeyote akiwaambia, 'Tazameni! Kristo huyu hapa,'[c] au, 'Pale!' msiamini.[d] **24** Kwa maana Makristo wa uwongo[e] na manabii wa uwongo[f] watatokea na kutoa ishara[g] kubwa na maajabu ili kuwapotosha, ikiwezekana, hata wale waliochaguliwa.[h] **25** Tazameni! Nimewaonya kimbele.[i] **26** Kwa hiyo, watu wakiwaambia ninyi, 'Tazameni! Yuko nyikani,' msiende; 'Tazameni! Yumo katika vyumba vya ndani,' msiamini.[j] **27** Kwa maana kama vile umeme[k] unavyotokea sehemu za mashariki na kuangaza mpaka sehemu za magharibi, ndivyo kuwapo kwa Mwana wa binadamu kutakavyokuwa.[l] **28** Popote mzoga ulipo, hapo ndipo watakapokusanyika[m] tai.[n]

29 "Mara baada ya ile dhiki ya siku hizo jua litatiwa giza,[o] nao mwezi[p] hautatoa nuru yake, nazo nyota zitaanguka kutoka mbinguni, nazo nguvu za mbingu zitatikiswa.[q] **30** Ndipo ishara ya Mwana wa binadamu[r] itakapoonekana mbinguni, ndipo makabila yote ya dunia yatakapojipiga-piga yenyewe kwa kuomboleza,[s] nayo yatamwona Mwana wa binadamu akija juu ya mawingu ya mbinguni akiwa na nguvu na utukufu mwingi.[t] **31** Naye atawatuma malaika zake pamoja na mvumo mkubwa wa

SURA 24

a Yoh 16:2 Mdo 7:59 Mdo 12:2 Ufu 6:11
b Mt 10:22 Yoh 15:21 Mdo 8:3
c Mk 13:9 Lu 21:12 2Ti 3:12 1Pe 2:21
d Mt 13:21
e Mt 10:21
f Mt 7:15 2Pe 2:1 1Yo 4:3
g Mdo 20:29 1Ti 4:1
h Mt 7:23 2Ti 3:2
i 2Th 2:10
j Ebr 10:36
k Mt 10:22 Ufu 2:10
l Isa 52:7 Mt 9:35 Kol 1:23
m Da 2:44 Mt 6:10
n Mt 28:19 Mk 13:10 Ro 10:18 Ufu 14:6
o Ufu 16:16 Ufu 19:19
p Kum 29:17 1Fa 11:5 Ufu 13:15
q Da 9:27 Da 11:31 Da 12:11 Mk 13:14
r Mwa 19:17 Lu 21:21
s Mk 13:17 Lu 21:23
t Ufu 7:14
u Da 12:1

Safu ya 2

a Isa 65:8 1Pe 2:9
b Mk 13:20
c Mt 24:5 Lu 17:23
d 1Yo 4:1
e 1Yo 2:18
f Kum 13:1 Mt 7:15 Mk 13:22 2Pe 2:1
g Mt 7:22 2Th 2:9 Ufu 13:13
h Mk 13:22
i Yoh 13:19
j Lu 17:23
k Ayu 37:3
l Da 7:13 Lu 17:24 1Ko 15:23 1Th 4:15
m Lu 17:37
n Ayu 39:30
o Yoe 2:31
p Ufu 6:12
q Mk 13:25 Lu 21:25 Ufu 6:13

r Da 7:13; Lu 21:27; s Zek 12:12; Ufu 1:7; t Da 7:14; Mt 26:64; Mk 13:26.

tarumbeta,[a] nao watawakusanya pamoja watu wake waliochaguliwa[b] kutoka kwenye zile pepo nne,[c] kutoka mwisho mmoja wa mbingu mpaka mwisho wake mwingine.

32 "Basi jifunzeni jambo hili kutokana na mtini kama mfano: Mara tu tawi lake changa linapokuwa jororo na kutoa majani, mnajua kwamba kiangazi kiko karibu.[d] **33** Vivyo hivyo ninyi pia, mnapoona mambo yote hayo, jueni kwamba yuko karibu milangoni.[e] **34** Kwa kweli ninawaambia ninyi kwamba kizazi hiki[f] hakitapitilia mbali kamwe mpaka mambo yote hayo yatukie. **35** Mbingu na dunia zitapitilia mbali,[g] lakini maneno yangu hayatapitilia mbali kamwe.[h]

36 "Kuhusu siku ile na saa[i] ile hakuna mtu anayejua, wala malaika wa mbinguni wala Mwana, ila Baba tu.[j] **37** Kwa maana kama vile siku za Noa[k] zilivyokuwa, ndivyo kuwapo kwa Mwana wa binadamu kutakavyokuwa.[l] **38** Kwa maana kama vile walivyokuwa katika siku hizo kabla ya gharika, wakila na kunywa, wanaume wakioa na wanawake wakiolewa, mpaka siku ambayo Noa[m] aliingia ndani ya safina;[n] **39** nao hawakujali mpaka gharika ikaja na kuwafagilia mbali wote,[o] ndivyo kuwapo kwa Mwana wa binadamu kutakavyokuwa. **40** Wakati huo watu wawili watakuwa shambani: mmoja atachukuliwa na mwingine ataachwa; **41** wanawake wawili watakuwa wakisaga kwenye jiwe la kusagia:[p] mmoja atachukuliwa na mwingine ataachwa.[a] **42** Kwa hiyo, endeleeni kukesha kwa sababu hamjui ni siku gani Bwana yenu atakuja.[b]

43 "Lakini jueni jambo moja, kwamba ikiwa mwenye nyumba angalijua mwizi anakuja katika kesha gani,[c] angaliendelea kukaa macho na hangaliruhusu nyumba yake ivunjwe. **44** Kwa hiyo ninyi pia iweni tayari,[d] kwa sababu Mwana wa binadamu atakuja katika saa msiyofikiria.

45 "Ni nani kwa kweli mtumwa mwaminifu na mwenye busara[e] ambaye bwana wake alimweka rasmi juu ya watumishi wake wa nyumbani, awape chakula chao kwa wakati unaofaa?[f] **46** Mtumwa huyo atakuwa mwenye furaha[g] ikiwa bwana wake atakapofika atamkuta akifanya hivyo! **47** Kwa kweli ninawaambia ninyi, Atamweka juu ya mali zake zote.[h]

48 "Lakini mtumwa huyo mwovu akisema moyoni mwake,[i] 'Bwana wangu anakawia,'[j] **49** naye aanze kuwapiga watumwa wenzake na kula na kunywa pamoja na walevi wa kupindukia, **50** bwana wa mtumwa huyo atakuja katika siku ambayo hatazamii na katika saa[k] ambayo hajui, **51** naye atamwadhibu kwa ukali[l] mkubwa zaidi na kumgawia sehemu yake pamoja na wanafiki. Huko ndiko atalia na kusaga meno.[m]

25 "Ndipo ufalme wa mbinguni utakuwa kama mabikira kumi waliochukua taa[n] zao na kwenda kumpo-

SURA 24
a Isa 27:13
b Ufu 7:3
c Mk 13:27
d Mk 13:28
Lu 21:30
e Yak 5:9
f Mt 23:36
g Ebr 1:11
h Mt 5:18
Lu 21:33
i Mdo 1:7
1Th 5:1
j Mk 13:32
k Mwa 6:11
Isa 54:9
l Mt 24:27
Lu 17:26
m Mwa 7:7
n Lu 17:27
Ebr 11:7
1Pe 3:20
2Pe 2:5
o Mwa 7:23
2Pe 3:6
p Isa 47:2

Safu ya 2
a Lu 17:35
b Mt 25:13
Mk 13:33
Lu 21:36
c Lu 12:39
1Th 5:2
2Pe 3:10
Ufu 3:3
d Mk 13:35
Lu 12:40
e 1Ko 4:2
Ebr 3:5
f Lu 12:42
g Ufu 16:15
h Mt 25:21
Lu 12:44
i Mhu 8:11
Ebr 3:12
j 2Pe 3:4
k Mt 25:13
l Lu 12:46
m Zb 112:10
Mt 8:12
Mt 25:30
Lu 13:28

SURA 25
n Lu 12:35
Flp 2:15

kea bwana-arusi.[a] **2** Watano
kati yao walikuwa wapumba-
vu,[b] na watano walikuwa we-
nye busara.[c] **3** Kwa maana
wale wapumbavu walichukua
taa zao lakini hawakuchukua
mafuta pamoja nao, **4** lakini
wale wenye busara walichukua
mafuta katika vyombo vyao
pamoja na taa zao. **5** Waka-
ti bwana-arusi alipokuwa ana-
kawia, wote walisinzia na ku-
anza kulala.[d] **6** Katikati ya
usiku kukatokea mwito,[e]
'Huyu hapa bwana-arusi! Ne-
ndeni mkampokee.' **7** Ndipo
mabikira wote hao wakasima-
ma na kuzitayarisha taa[f] zao.
8 Wale wapumbavu wakawaam-
bia wale wenye busara, 'Tu-
peni sisi kiasi fulani cha ma-
futa[g] yenu, kwa sababu taa
zetu zinakaribia kuzimika.'
9 Wale wenye busara[h] waka-
wajibu kwa maneno haya, 'Lab-
da huenda tusiwe na ya kuto-
sha kwa ajili yetu na kwa aji-
li yenu. Badala yake, shikeni
njia mwende kwa wale wanao-
yauza mkajinunulie.' **10** Wa-
lipokuwa wakienda zao kunu-
nua, bwana-arusi akafika, na
wale mabikira waliokuwa taya-
ri wakaingia pamoja naye kwe-
nye karamu ya arusi;[i] nao mla-
ngo ukafungwa. **11** Baadaye
wale mabikira wengine pia wa-
kaja, wakisema, 'Bwana, bwa-
na, tufungulie!'[j] **12** Akajibu,
akasema, 'Ninawaambia ninyi
kweli, Siwajui ninyi.'[k]

13 "Kwa hiyo, endeleeni ku-
kesha[l] kwa sababu hamwijui
ile siku wala saa.[m]

14 "Kwa maana ni kama wa-
kati ambapo mtu,[n] akiwa ka-
ribu kusafiri ng'ambo,[o] aliwai-

SURA 25

a Yoh 3:29
Ufu 19:7
b Mt 7:26
c Mt 7:24
d 1Th 5:6
e Mt 24:31
f Lu 12:35
g Ebr 1:9
h Mt 7:24
i Ufu 19:9
j Lu 13:25
Ebr 12:17
k Lu 13:27
l 1Th 5:6
1Pe 5:8
m Mt 24:42
Mt 24:50
Mk 13:33
n Lu 19:12
o Mt 21:33

Safu ya 2

a Lu 19:13
b Ro 12:6
c Met 10:4
d Mt 24:48
e Mt 18:23
Lu 19:15
f Lu 19:16
g Lu 19:17
h Met 28:20
Lu 16:10
i Met 12:24
Lu 12:44
j Ebr 12:2
k Lu 19:18
l Lu 19:19
m Ebr 12:2

ta watumwa wake na kuwa-
pa mali zake.[a] **15** Akampa
mmoja talanta tano, mwingi-
ne mbili, na mwingine moja,
kila mmoja kulingana na
uwezo wake mwenyewe,[b] naye
akaenda ng'ambo. **16** Mara
moja yule aliyezipokea tala-
nta tano akaenda zake na ku-
fanya biashara nazo na kupata
faida ya tano zaidi.[c] **17** Vi-
vyo hivyo yule aliyepokea mbi-
li akapata faida ya mbili za-
idi. **18** Lakini yule aliyepo-
kea moja tu akaenda zake, na
kuchimba katika udongo na
kuficha zile fedha za bwana
wake.

19 "Baada ya muda mrefu[d]
bwana wa watumwa hao aliku-
ja na kufanya hesabu pamoja
nao.[e] **20** Kwa hiyo yule aliye-
kuwa amepokea talanta tano
akaja na kuleta talanta tano
zaidi, akisema, 'Bwana, ulini-
pa talanta tano; ona, nilipa-
ta faida ya talanta tano zaidi.'[f]
21 Bwana wake akamwambia,
'Vema, mtumwa mwema na
mwaminifu![g] Ulikuwa mwami-
nifu[h] juu ya mambo machache.
Nitakuweka juu ya mambo
mengi.[i] Ingia katika shangwe[j]
ya bwana wako.' **22** Halafu
yule aliyekuwa amepokea ta-
lanta mbili akaja na kusema,
'Bwana, ulinipa talanta mbili;
ona, nilipata faida ya talanta
mbili zaidi.'[k] **23** Bwana wake
akamwambia, 'Vema, mtumwa
mwema na mwaminifu! Uliku-
wa mwaminifu juu ya mambo
machache. Nitakuweka juu ya
mambo mengi.[l] Ingia katika
shangwe[m] ya bwana wako.'

24 "Mwishowe yule aliye-
kuwa amepokea talanta moja

akaja[a] na kusema, 'Bwana nilijua wewe ni mtu mwenye
kudai, ambaye huvuna mahali ambapo hukupanda na kukusanya mahali ambapo hukupepeta. **25** Kwa hiyo nikaogopa[b] na kwenda zangu
na kuficha talanta yako katika udongo. Tazama, hiki hapa
kilicho chako.' **26** Bwana wake akamjibu, akamwambia,
'Mtumwa mwovu na goigoi, ulijua, sivyo, kwamba mimi nilivuna mahali ambapo sikupanda na kukusanya mahali
ambapo sikupepeta? **27** Hivyo, basi, ulipaswa kuwa umeweka fedha zangu kwa wenye
kutunza akiba, na wakati wa kufika kwangu ningekuwa nikipokea kilicho changu pamoja na faida.[c]

28 "'Kwa hiyo ichukueni talanta hiyo kutoka kwake na
kumpa yule aliye na talanta kumi.[d] **29** Kwa maana kila
mtu aliye na kitu, ataongezewa naye atakuwa na vingi; lakini yule ambaye hana kitu, hata
kile alicho nacho kitachukuliwa.[e] **30** Nanyi mtupeni nje
katika giza mtumwa huyo asiyefaa kitu. Huko ndiko atalia
na kusaga meno yake.'[f]

31 "Wakati Mwana wa binadamu[g] atakapofika katika utukufu wake, na malaika wote pamoja naye,[h] ndipo atakapoketi juu ya kiti chake cha ufalme
chenye utukufu.[i] **32** Na mataifa yote yatakusanyika mbele yake,[j] naye atawatenganisha watu,[k] mmoja kutoka kwa
mwenzake,[l] kama vile mchungaji anavyotenganisha kondoo na mbuzi. **33** Naye atawaweka kondoo kwenye mkono wake wa kuume,[a] lakini
mbuzi kwenye mkono wake wa kushoto.[b]

34 "Ndipo mfalme atakapowaambia wale walio kwenye
mkono wake wa kuume, 'Njooni, ninyi ambao mmebarikiwa na Baba yangu,[c] urithini[d] ufalme[e] uliotayarishwa kwa ajili
yenu tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu.[f] **35** Kwa maana nilikuwa mwenye njaa nanyi mkanipa chakula;[g] nilikuwa na kiu nanyi mkanipa kinywaji. Nilikuwa mgeni nanyi
mkanikaribisha;[h] **36** nilikuwa uchi,[i] nanyi mkanivika. Nilishikwa na ugonjwa nanyi mkanitunza. Nilikuwa gerezani[j] nanyi mkanijia.' **37** Ndipo waadilifu watamjibu kwa
maneno haya, 'Bwana, ni wakati gani tulipokuona ukiwa
na njaa na kukulisha, au ukiwa na kiu,[k] na kukupa kinywaji?[l] **38** Ni wakati gani tulipokuona ukiwa mgeni na kukukaribisha, au ukiwa uchi,
na kukuvika? **39** Ni wakati gani tulipokuona ukiwa mgonjwa au gerezani na kukujia?'
40 Na mfalme[m] atajibu na kuwaambia, 'Kwa kweli ninawaambia ninyi, Kwa kadiri ambayo mlimtendea hilo mmoja wa
walio wadogo zaidi[n] wa ndugu zangu[o] hawa, mlinitendea
mimi.'[p]

41 "Ndipo naye atawaambia, wale walio kwenye mkono wake
wa kushoto, 'Tokeni kwangu mwende zenu,[q] ninyi ambao
mmelaaniwa, mkaingie katika moto wa milele[r] aliotayarishiwa Ibilisi na malaika zake.[s]
42 Kwa maana nilikuwa na njaa, lakini hamkunipa cha-

SURA 25

a Lu 19:20
b Met 26:13
Lu 19:21
Ufu 21:8
c Lu 19:23
d Lu 19:24
e Mt 13:12
Mk 4:25
Lu 8:18
Yoh 15:2
f Zb 112:10
Mt 8:12
g Da 7:13
Mt 16:27
Mdo 1:11
Ufu 1:7
h Zek 14:5
Mt 13:41
Mt 19:28
i Ufu 3:21
j 2Ko 5:10
k Eze 34:17
Mt 13:49
l Eze 20:38

Safu ya 2

a Yoh 10:16
b Mt 25:41
c Zb 115:15
d Ro 8:17
e 1Th 2:12
Ufu 5:10
f Mt 13:35
Ebr 9:26
1Pe 1:20
Ufu 13:8
g Isa 58:7
Eze 18:16
h Ebr 13:2
3Yo 5
i Eze 18:7
Yak 2:15
j 2Ti 1:16
k Mt 10:42
l Mt 6:3
m Lu 19:38
Ufu 17:14
n Met 19:17
Mt 10:40
Mk 9:41
o 2Ko 5:20
Ebr 2:11
p Ebr 6:10
q Mt 7:23
Lu 13:27
r Mt 18:8
Ufu 20:10
s Ufu 12:9

kula chochote,[a] nami nilikuwa na kiu,[b] lakini hamkunipa kinywaji chochote. **43** Nilikuwa mgeni, lakini hamkunikaribisha; nilikuwa uchi, lakini hamkunivika;[c] nilikuwa mgonjwa na gerezani,[d] lakini hamkunitunza.' **44** Ndipo wao pia watamjibu kwa maneno haya, 'Bwana, ni wakati gani tulipokuona ukiwa na njaa au ukiwa na kiu au ukiwa mgeni au ukiwa uchi au mgonjwa au gerezani na tukakosa kukuhudumia?' **45** Ndipo atawajibu wao kwa maneno haya, 'Kwa kweli ninawaambia ninyi, Kwa kadiri ambayo hamkumtendea hilo mmoja wa hawa wadogo zaidi,[e] hamkunitendea[f] mimi.'[g] **46** Na hawa watakatiliwa mbali milele,[h] lakini waadilifu wataingia katika uzima wa milele."[i]

26 Basi Yesu alipokuwa amemaliza kusema yote hayo, aliwaambia wanafunzi wake: **2** "Mnajua kwamba siku mbili tangu sasa kutakuwa na pasaka,[j] naye Mwana wa binadamu atatolewa ili atundikwe mtini."[k]

3 Ndipo wakuu wa makuhani na wanaume wazee wa watu wakakusanyika pamoja katika ua wa kuhani mkuu aliyeitwa Kayafa,[l] **4** na kushauriana[m] pamoja ili wamkamate Yesu kwa hila na kumuua. **5** Hata hivyo, wao wakawa wakisema: "Si kwenye sherehe, ili ghasia zisitokee katikati ya watu."[n]

6 Ikawa kwamba Yesu alipokuwa Bethania[o] katika nyumba ya Simoni mwenye ukoma,[p] **7** mwanamke mwenye chupa ya alabasta iliyo na mafuta ghali yenye marashi[a] akamkaribia, naye akaanza kuyamimina juu ya kichwa cha Yesu alipokuwa ameketi mezani. **8** Walipoona hilo wanafunzi wakaghadhibika na kusema: "Hasara hii ni ya nini?[b] **9** Kwa maana yangaliweza kuuzwa kwa kiasi kikubwa na kupewa maskini."[c] **10** Akijua jambo hilo,[d] Yesu akawaambia: "Kwa nini mnataka kumsumbua mwanamke huyu? Kwa kuwa amenitendea tendo jema.[e] **11** Kwa maana ninyi mna maskini[f] pamoja nanyi sikuzote, lakini hamtakuwa pamoja nami sikuzote.[g] **12** Kwa kuwa mwanamke huyu alipotia mafuta haya yenye marashi juu ya mwili wangu, alifanya hivyo ili kunitayarisha kwa ajili ya maziko.[h] **13** Kwa kweli ninawaambia ninyi, Kokote ambako hii habari njema itahubiriwa katika ulimwengu wote, jambo ambalo mwanamke huyu ametenda litasimuliwa pia kuwa kumbukumbu lake."[i]

14 Ndipo mmoja wa wale kumi na wawili, anayeitwa Yuda Iskariote,[j] akaenda kwa wakuu wa makuhani **15** na kusema: "Mtanipa nini ili nimsaliti kwenu?"[k] Wakamwagizia vipande 30 vya fedha.[l] **16** Kwa hiyo tangu wakati huo na kuendelea akawa akitafuta nafasi nzuri ya kumsaliti.[m]

17 Katika siku ya kwanza ya keki zisizo na chachu[n] wanafunzi wakamjia Yesu, wakisema: "Ni wapi unapotaka tukutayarishie uile pasaka?"[o] **18** Akasema: "Nendeni jijini

SURA 25
a Isa 58:7 Eze 18:16
b Mt 10:42
c Eze 18:7 Yak 2:15
d 2Ti 1:16
e Kum 23:4 2Ko 5:20 Ebr 2:11
f Zek 2:8
g Mdo 9:5
h Da 12:2 2Pe 2:9
i Ro 2:7

SURA 26
j Kut 12:14 Mk 14:1 Lu 22:1 Yoh 13:1
k Mt 16:21 Mt 20:19 Mt 27:26 Mk 15:15 Yoh 19:16
l Mt 26:57 Lu 3:2 Lu 22:2 Yoh 18:13 Yoh 18:24
m Zb 2:2 Mk 14:1 Yoh 11:49
n Mk 14:2
o Mt 21:17
p Mt 8:2

Safu ya 2
a Mk 14:3 Yoh 12:3
b Mk 14:4 Yoh 12:4
c Mk 14:5 Yoh 12:5
d Yoh 12:6
e Mk 14:6
f Kum 15:11 Mk 14:7
g Mt 9:15 Yoh 12:8 Yoh 17:11
h Mk 14:8 Yoh 12:7
i Mk 14:9
j Mt 10:4 Lu 22:3 Yoh 13:2
k Mk 14:10 Yoh 11:57 1Ti 6:10
l Kut 21:32 Zek 11:12 Mt 27:3 Mk 14:11 Lu 22:5
m Mk 14:11 Lu 22:6
n Kut 12:18 Kut 23:15 Law 23:6 Mk 14:12 Lu 22:7
o Lu 22:9

kwa Fulani-wa-fulani,[a] mka-
mwambie, Mwalimu anasema,
'Wakati wangu uliowekwa uko
karibu; nitasherehekea pasaka
pamoja na wanafunzi wangu
nyumbani mwako.'"[b] **19** Nao
wanafunzi wakafanya kama
Yesu alivyowaagiza, nao waka-
tayarisha vitu kwa ajili ya pa-
saka.[c]

20 Basi, ilipofika jioni,[d] ali-
kuwa ameketi mezani pamoja
na wale wanafunzi kumi na wa-
wili.[e] **21** Walipokuwa wakila,
alisema: "Kwa kweli ninawaa-
mbia ninyi, Mmoja wenu ata-
nisaliti."[f] **22** Wakiwa wame-
huzunishwa sana na jambo
hilo, kila mmoja wao akaa-
nza kumwambia: "Bwana, je,
ni mimi?"[g] **23** Akajibu, aka-
sema: "Yule anayechovya mko-
no wake pamoja nami kati-
ka bakuli ndiye atakayenisali-
ti.[h] **24** Kwa kweli, Mwana
wa binadamu anaenda zake,
kama ilivyoandikwa[i] kumhu-
su, lakini ole[j] wake mtu yule
ambaye kupitia kwake Mwa-
na wa binadamu atasalitiwa![k]
Ingalikuwa afadhali kwake
kama mtu huyo asingalizali-
wa." **25** Yuda, aliyekuwa ka-
ribu kumsaliti, akajibu, akase-
ma: "Je, ni mimi, Rabi?" Aka-
mwambia: "Wewe mwenyewe
umesema."

26 Walipokuwa wakiende-
lea kula, Yesu alichukua mka-
te[l] na, baada ya kutoa baraka,
akaumega,[m] akawapa wanafu-
nzi, akasema: "Chukueni, mle.
Huu unamaanisha mwili wa-
ngu."[n] **27** Pia, akachukua ki-
kombe[o] na, akiisha kushukuru,
akawapa, akisema: "Kinywee-
ni, ninyi nyote;[p] **28** kwa maa-

SURA 26

a Mt 21:3
Mk 14:13
Lu 22:10
b Mk 14:14
Lu 22:11
c Mk 14:16
Lu 22:13
d Kum 16:6
e Mk 14:17
Lu 22:14
f Mk 14:18
Yoh 6:70
Yoh 13:21
g Mk 14:19
Yoh 13:22
h Zb 41:9
Mk 14:20
Lu 22:21
Yoh 13:26
i Mt 5:17
j Kum 27:25
Lu 22:22
k Mk 14:21
Yoh 17:12
l 1Ko 11:23
m 1Ko 10:16
1Ko 11:24
n Mk 14:22
Lu 22:19
o 1Ko 11:25
p Lu 22:20

Safu ya 2

a 1Ko 10:16
b Kut 24:8
Zek 9:11
c Yer 31:31
Ebr 7:22
Ebr 9:20
d Mt 20:28
Mk 14:24
e Efe 1:7
Ebr 9:22
f Lu 22:18
g Zb 113:1-9
h Lu 22:39
Yoh 18:1
i Zek 13:7
Mk 14:27
Yoh 16:32
j Mt 28:7
Mt 28:16
k Met 11:2
Mk 14:29
l Mk 14:30
Lu 22:34
Yoh 13:38
m Mk 14:31
Lu 22:33
n Lu 22:39
Yoh 18:1
o Mk 14:32
Lu 22:40
p Mk 5:37
q Isa 53:3
Mk 14:33

na hii inamaanisha[a] 'damu[b]
yangu ya agano,'[c] ambayo
itamwagwa kwa ajili ya we-
ngi[d] kwa msamaha wa dhambi.[e]
29 Lakini ninawaambia ninyi,
Tangu sasa sitakunywa ka-
mwe divai yoyote ya mzabi-
bu mpaka siku ile nitaka-
pokunywa ikiwa mpya, pamo-
ja nanyi katika ufalme wa Baba
yangu."[f] **30** Mwishowe, baa-
da ya kuimba sifa,[g] wakato-
ka na kwenda kwenye Mlima
wa Mizeituni.[h]

31 Ndipo Yesu akawaambia:
"Ninyi nyote mtakwazika ku-
husiana nami usiku huu,
kwa maana imeandikwa, 'Nita-
mpiga mchungaji, nao kon-
doo wa kundi watatawa-
nyika huku na huku.'[i] **32** La-
kini baada ya kufufuliwa
nitawatangulia kuingia Gali-
laya."[j] **33** Lakini Petro akaji-
bu, akamwambia: "Ijapoku-
wa wengine wote wakwazi-
ke kuhusiana nawe, mimi sita-
kwazika kamwe!"[k] **34** Yesu
akamwambia: "Kwa kweli ni-
nakuambia wewe, Usiku huu,
kabla ya jogoo kuwika, uta-
nikana mara tatu."[l] **35** Petro
akamwambia: "Hata nikilazi-
mika kufa pamoja nawe, mimi
sitakukana kamwe." Wale wa-
nafunzi wengine wote wakase-
ma vivyo hivyo pia.[m]

36 Ndipo Yesu akaja pamo-
ja nao mpaka mahali[n] pana-
poitwa Gethsemane, naye
akawaambia wanafunzi: "Ke-
tini hapa ninapoenda pale na
kusali."[o] **37** Naye akawachu-
kua Petro na wale wana wawi-
li[p] wa Zebedayo pamoja naye,
akaanza kuhuzunika na ku-
taabika sana.[q] **38** Ndipo aka-

waambia: "Nafsi yangu ina huzuni sana, kiasi cha kufa.[a] Kaeni hapa na mwendelee kukesha pamoja nami."[b] **39** Naye akasonga mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akasali[c] na kusema: "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki[d] na kipitilie mbali kutoka kwangu. Lakini, si kulingana na mapenzi yangu,[e] bali kulingana na mapenzi yako."[f]

40 Naye akaja walipokuwa wanafunzi na kuwakuta wamelala usingizi, naye akamwambia Petro: "Je, hamngeweza kukesha hata saa moja pamoja nami?[g] **41** Endeleeni kukesha[h] na kusali[i] sikuzote, ili msiingie katika jaribu.[j] Bila shaka, roho inataka, lakini mwili ni dhaifu."[k] **42** Tena, kwa mara ya pili,[l] akaenda zake na kusali, akisema: "Baba yangu, ikiwa haiwezekani kipitilie mbali ila nikinywe, acha mapenzi yako yatendeke."[m] **43** Naye akaja tena na kuwakuta wamelala usingizi, kwa maana macho yao yalikuwa mazito.[n] **44** Kwa hiyo akawaacha, akaenda zake tena na kusali kwa mara ya tatu,[o] akisema mara moja tena neno lilelile. **45** Kisha akaja walipokuwa wanafunzi na kuwaambia: "Wakati kama huu ninyi mnalala usingizi na kupumzika! Tazameni! Saa imekaribia Mwana wa binadamu asalitiwe na kutiwa katika mikono ya watenda-dhambi.[p] **46** Simameni, twende. Tazama! Msaliti wangu amekaribia."[q] **47** Na alipokuwa bado akisema, tazama! Yuda,[r] mmoja wa wale kumi na wawili, akaja pamoja na umati mkubwa ukiwa na mapanga[a] na marungu kutoka kwa wakuu wa makuhani na wanaume wazee wa watu.[b]

48 Basi msaliti wake alikuwa amewapa ishara, akisema: "Yeyote yule nitakayembusu, huyo ndiye; mkamateni."[c] **49** Naye akaenda moja kwa moja kwa Yesu akasema: "Siku njema, Rabi!"[d] na kumbusu[e] kwa wororo sana. **50** Lakini Yesu[f] akamwambia: "Mwenzangu, uko hapa kwa kusudi gani?" Ndipo wakaja wakaweka mikono juu ya Yesu na kumkamata.[g] **51** Lakini, tazama! mmoja wa wale waliokuwa pamoja na Yesu akanyoosha mkono wake akauchomoa upanga wake, akampiga mtumwa wa kuhani mkuu akalikata sikio lake.[h] **52** Ndipo Yesu akamwambia: "Rudisha upanga wako mahali pake,[i] kwa maana wale wote wanaouchukua upanga wataangamia kwa upanga.[j] **53** Au unafikiri kwamba siwezi kumwomba Baba yangu anipe sasa hivi vikosi zaidi ya kumi na viwili vya malaika?[k] **54** Hata hivyo, Maandiko yangetimizwaje kwamba lazima itendeke hivi?" **55** Ndipo Yesu akauambia umati: "Je, mmetoka mkiwa na mapanga na marungu kana kwamba ni kwenda juu ya mnyang'anyi ili kunikamata?[l] Siku baada ya siku nilikuwa nikiketi katika hekalu[m] nikifundisha, na bado hamkunikamata. **56** Lakini yote haya yametukia ili maandiko ya manabii yatimizwe."[n] Ndipo wanafunzi wote wakamwacha na kukimbia.[o]

SURA 26

a Zb 42:11
Zb 43:5
b Mk 14:34
c Ebr 5:7
d Mt 20:22
Yoh 18:11
e Yoh 5:30
Yoh 6:38
f Zb 40:8
Mk 14:36
Lu 22:42
Ebr 10:9
g Mk 14:37
Lu 22:45
h Mk 13:33
1Pe 5:8
Ufu 16:15
i Lu 18:1
Ro 12:12
Efe 6:18
1Pe 4:7
j Mt 6:13
Lu 22:46
k Mk 14:38
Ro 7:23
Ga 5:17
l Mk 14:39
m Mt 6:10
Yoh 12:27
Mdo 21:14
n Mk 14:40
o 2Ko 12:8
p Mk 14:41
q Mk 14:42
r Lu 22:47
Yoh 18:3

Safu ya 2

a Lu 22:52
Mdo 1:16
b Mk 14:43
c Mk 14:44
d Mk 14:45
e 2Sa 20:9
Met 27:6
f Lu 22:48
g Zb 41:9
Mk 14:46
h Mk 14:47
Lu 22:50
Yoh 18:10
i Yoh 18:11
j Mwa 9:6
Ufu 13:10
k 2Fa 6:17
Da 7:10
Mt 4:11
l Mk 14:48
Lu 22:52
m Lu 19:47
Yoh 18:20
n Zb 22:Uta-31
Isa 53:1-12
Omb 4:20
Da 9:26
o Zek 13:7
Mk 14:50
Yoh 16:32

57 Wale waliomkamata Yesu
wakampeleka kwa Kayafa[a] ku-
hani mkuu, ambako waandi-
shi na wanaume wazee wali-
kuwa wamekusanywa pamo-
ja.[b] **58** Lakini Petro akaen-
delea kumfuata akiwa mbali
kiasi, mpaka katika ua[c] wa ku-
hani mkuu, na, baada ya kui-
ngia ndani, akaketi pamoja na
watumishi wa nyumbani ili ku-
ona matokeo.[d]
59 Wakati huohuo wakuu
wa makuhani na Sanhedri-
ni nzima walikuwa wakitafu-
ta ushahidi wa uwongo juu
ya Yesu ili wamuue,[e] **60** laki-
ni hawakupata wowote, ija-
pokuwa mashahidi wengi wa
uwongo walijitokeza.[f] Baadaye
wawili wakajitokeza **61** na
kusema: "Mtu huyu alisema,
'Ninaweza kuliangusha chini
hekalu la Mungu na kulijenga
katika siku tatu.'"[g] **62** Ndipo
kuhani mkuu akasimama na
kumwambia: "Je, huna jibu?
Watu hawa wanashuhudia nini
juu yako?"[h] **63** Lakini Yesu
akaendelea kukaa kimya.[i]
Kwa hiyo kuhani mkuu aka-
mwambia: "Kwa Mungu aliye
hai ninakuweka chini ya kia-
po[j] utuambie kama wewe ndi-
ye Kristo[k] Mwana wa Mungu!"
64 Yesu akamwambia:[l] "Wewe
mwenyewe umesema.[m] Laki-
ni ninawaambia ninyi, Tangu
sasa[n] mtamwona Mwana wa bi-
nadamu[o] akiwa ameketi kwe-
nye mkono wa kuume[p] wa ngu-
vu na akija juu ya mawingu
ya mbinguni."[q] **65** Ndipo ku-
hani mkuu akayararua mava-
zi yake ya nje, akisema: "Ame-
kufuru![r] Tunahitaji mashahi-
di wengine wa nini?[s] Tazama!
Sasa mmelisikia kufuru.[a]
66 Mnaonaje?" Wakamjibu:
"Anastahili kufa."[b] **67** Ndi-
po wakamtemea mate usoni[c]
na kumpiga[d] ngumi. Wengi-
ne wakampiga makofi usoni,[e]
68 wakisema: "Tutolee unabii,
wewe Kristo.[f] Ni nani aliyeku-
piga?"[g]
69 Basi Petro alikuwa ame-
keti nje katika ua; na mjaka-
zi akamjia, akisema: "Wewe,
pia, ulikuwa pamoja na Yesu
Mgalilaya!"[h] **70** Lakini aka-
kana mbele yao wote, akisema:
"Sijui unalosema." **71** Alipo-
kuwa amekwisha kutoka na
kwenda kwenye chumba kili-
cho langoni, msichana mwingi-
ne alimwona na kuwaambia
wale waliokuwa hapo: "Mtu
huyu alikuwa pamoja na Yesu
Mnazareti."[i] **72** Naye akaka-
na tena, kwa kiapo: "Si-
mjui mtu huyo!"[j] **73** Baada
ya muda kidogo wale walio-
kuwa wamesimama kuzungu-
ka wakaja na kumwambia Pe-
tro: "Hakika wewe pia ni mmo-
ja wao, kwa maana, kwa kweli,
matamshi yako yanakutambu-
lisha wazi."[k] **74** Ndipo akaan-
za kulaani na kuapa: "Simjui
mtu huyo!" Na mara jogoo aka-
wika.[l] **75** Naye Petro akaku-
mbuka maneno ambayo Yesu
alisema, yaani: "Kabla ya jo-
goo kuwika, utanikana mara
tatu."[m] Naye akaenda nje aka-
lia kwa uchungu.[n]

27 Asubuhi ilipofika, wa-
kuu wote wa makuha-
ni na wanaume wazee wa watu
wakashauriana juu ya Yesu ili
auawe.[o] **2** Na, baada ya ku-
mfunga, wakampeleka na ku-

SURA 26
a Mk 14:53
Yoh 18:13
b Lu 22:54
c Lu 22:55
d Yoh 18:16
e Kut 20:16
Mk 14:55
f Kum 19:15
Zb 27:12
Zb 35:11
Mk 14:57
g Mt 27:40
Yoh 2:19
Mdo 6:14
h Mk 14:60
i Met 11:12
Isa 53:7
Mdo 8:32
j 1Fa 22:16
k Mt 16:16
Lu 22:67
Yoh 10:24
l Mk 14:62
m Lu 22:70
n Lu 22:69
o Yoh 1:51
p Zb 110:1
Da 7:14
Lu 22:69
q Da 7:13
Mk 14:62
Ufu 1:7
r Mk 14:63
s Lu 22:71

Safu ya 2
a Mk 14:64
b Law 24:16
Yoh 19:7
c Isa 50:6
Mt 27:30
Mk 14:65
d Lu 22:63
e Isa 53:3
Yoh 19:3
f Lu 23:39
g Mk 14:65
Lu 22:64
h Lu 22:57
Yoh 18:17
i Mk 14:67
Yoh 18:25
j Lu 22:58
k Amu 12:6
Lu 22:59
Yoh 18:26
l Lu 22:60
Yoh 18:27
m Mt 26:34
Mk 14:30
Yoh 13:38
n Mk 14:72
Lu 22:62

SURA 27
o Zb 2:2
Mk 15:1
Lu 22:66
Yoh 18:28

mtia mkononi mwa gavana
Pilato.[a]
3 Ndipo Yuda, aliyemsaliti,
alipoona kuwa amekwisha ku-
hukumiwa adhabu, akajuta,
akavirudisha vile vipande 30[b]
vya fedha kwa wakuu wa ma-
kuhani na wanaume wazee,
4 akisema: "Nilitenda dhambi
niliposaliti damu yenye ua-
dilifu."[c] Wakasema: "Hilo li-
natuhusu nini? Shauri yako!"[d]
5 Basi akatupa vile vipa-
nde vya fedha hekaluni aka-
ondoka, akaenda zake akaji-
nyonga.[e] **6** Lakini wakuu wa
makuhani wakavichukua hi-
vyo vipande vya fedha na ku-
sema: "Si halali kuvitumbuki-
za katika hazina takatifu, kwa
sababu hivyo ni bei ya damu."
7 Baada ya kushauriana pa-
moja, wakavitumia kununua
shamba la mfinyanzi ili ku-
zikia wageni. **8** Kwa hiyo
shamba hilo limeitwa "Sha-
mba la Damu"[f] mpaka leo hii.
9 Ndipo likatimizwa lililose-
mwa kupitia nabii Yeremia,
akisema: "Nao walichukua vile
vipande 30 vya fedha,[g] amba-
vyo ni bei juu ya mtu aliyepi-
gwa bei, ambaye baadhi ya
wana wa Israeli walimpigia bei,
10 nao wakavitoa kwa ajili ya
shamba la mfinyanzi,[h] kulinga-
na na lile ambalo Yehova aliku-
wa ameniamuru."
11 Yesu sasa akasimama
mbele ya gavana; naye gava-
na akamuuliza: "Je, wewe
ndiye mfalme wa Wayahu-
di?"[i] Yesu akajibu: "Wewe mwe-
nyewe unasema."[j] **12** Laki-
ni, alipokuwa akishtakiwa[k]
na wakuu wa makuhani na
wanaume wazee, hakujibu.[l]

SURA 27
a Mt 20:19
Lu 23:1
Yoh 18:28
Mdo 3:13
b Mt 26:15
Mk 14:11
c Kum 19:10
2Fa 24:4
d Mt 27:24
Ebr 10:26
e 2Sa 17:23
Zb 55:23
Mdo 1:18
f Mdo 1:19
g Zek 11:12
h Zek 11:13
i Mk 15:2
Lu 23:3
Yoh 18:33
j Mt 26:64
1Ti 6:13
k Mk 15:3
l Met 11:12
Isa 53:7
Mt 26:63
Yoh 19:9

Safu ya 2
a Mk 15:4
b Mk 15:5
c Lu 23:17
Yoh 18:39
d Lu 23:19
Yoh 18:40
e Mk 15:9
f Mk 15:10
g Met 27:4
Yoh 12:19
Ro 1:29
h Isa 53:11
Zek 9:9
1Yo 2:1
i Mt 2:12
j Lu 23:18
Yoh 18:40
Mdo 3:14
k Mk 15:11
l Mk 15:13
Lu 23:21
m Mk 15:14
Lu 23:23
Mdo 3:13

13 Ndipo Pilato akamwambia:
"Je, husikii ni mambo manga-
pi wanashuhudia juu yako?"[a]
14 Lakini hakumjibu, hata
neno moja, hivi kwamba gava-
na akastaajabu sana.[b]
15 Sasa kutoka sherehe mpa-
ka sherehe ilikuwa desturi ya
gavana kufungulia umati mfu-
ngwa mmoja, ambaye walimta-
ka.[c] **16** Wakati huohuo wali-
kuwa wamemshika mfungwa
mwenye sifa mbaya anayeit-
wa Baraba.[d] **17** Kwa saba-
bu hiyo walipokuwa wameku-
sanywa pamoja Pilato akawa-
ambia: "Mnataka niwafungulie
nani, Baraba au Yesu anayeit-
wa Kristo?"[e] **18** Kwa maa-
na alijua kwamba walikuwa
wamemtia mikononi mwake[f]
kwa sababu ya wivu.[g] **19** Zai-
di ya hayo, alipokuwa ameke-
ti juu ya kiti cha hukumu, mke
wake akampelekea habari, aki-
sema: "Usijihusishe kamwe na
mtu huyo mwadilifu,[h] kwa maa-
na niliteseka sana leo kati-
ka ndoto[i] kwa sababu yake."
20 Lakini wakuu wa makuha-
ni na wanaume wazee wakau-
shawishi umati uombe wapewe
Baraba,[j] lakini Yesu aangami-
zwe. **21** Sasa gavana akajibu,
akawaambia: "Mnataka niwa-
fungulie nani kati ya hawa wa-
wili?" Wakasema: "Baraba."[k]
22 Pilato akawaambia: "Basi,
nitafanya nini na Yesu anayeit-
wa Kristo?" Wote wakasema:
"Atundikwe mtini!"[l] **23** Aka-
sema: "Kwani, amefanya jambo
gani baya?" Bado wao wakaen-
delea kupaaza sauti hata zai-
di: "Atundikwe mtini!"[m]
24 Alipoona kwamba hai-
kufaidi kitu bali, badala yake,

ghasia zilikuwa zikitokea, Pilato alichukua maji[a] na kunawa mikono yake mbele ya ule umati, akisema: "Mimi sina hatia ya damu ya mtu huyu. Shauri yenu." **25** Ndipo watu wote wakajibu, wakasema: "Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu."[b] **26** Ndipo akawafungulia Baraba, lakini akaagiza Yesu apigwe mijeledi[c] na kumtoa ili atundikwe mtini.[d]

27 Ndipo askari-jeshi wa gavana wakampeleka Yesu ndani ya jumba la gavana na kukusanya pamoja kikosi chote cha askari kwake.[e] **28** Nao wakamvua kanzu yake, wakampamba kwa joho jekundu,[f] **29** nao wakasokota taji kutokana na miiba na kuliweka juu ya kichwa chake na utete katika mkono wake wa kuume. Nao wakapiga magoti mbele yake, wakamfanyia dhihaka,[g] wakisema: "Siku njema, ewe Mfalme wa Wayahudi!"[h] **30** Nao wakamtemea mate[i] na kuuchukua ule utete na kuanza kumpiga kichwani. **31** Mwishowe, walipokuwa wamemdhihaki,[j] wakalivua lile joho na kumvika mavazi yake ya nje na kumpeleka akatundikwe mtini.[k]

32 Walipokuwa wakiondoka walimkuta mzaliwa wa Kirene anayeitwa Simoni.[l] Wakamlazimisha aubebe mti wake wa mateso. **33** Nao walipofika mahali panapoitwa *Golgotha,*[m] ndiyo kusema, Mahali pa Fuvu la Kichwa, **34** wakampa divai iliyochanganywa na nyongo[n] anywe; lakini, baada ya kuionja, akakataa kuinywa.[o]

SURA 27

a Kum 21:6
b Kum 19:10
Yos 2:19
Mdo 5:28
1Th 2:15
c Lu 18:33
Yoh 19:1
d Mk 15:15
Lu 23:25
e Mk 15:16
f Yoh 19:2
g Amu 16:25
h Mk 15:19
Yoh 19:3
i Isa 49:7
Isa 50:6
Mt 26:67
j Isa 53:7
Mt 20:19
k Mk 15:20
l Mk 15:21
Lu 23:26
Yoh 19:17
m Lu 23:33
Yoh 19:17
n Zb 69:21
o Mk 15:23

Safu ya 2

a Zb 22:16
Yoh 19:18
b Zb 22:18
Lu 23:34
Yoh 19:23
c Mk 15:24
d Mk 15:26
Lu 23:38
Yoh 19:19
e Isa 53:12
Mk 15:27
Lu 23:33
Yoh 19:18
f Lu 18:32
Ebr 12:3
g Zb 22:7
Zb 109:25
Lu 23:35
h Mt 26:61
Yoh 2:19
i Mk 15:30
Lu 4:3
j Mk 15:31
Lu 23:35
k Yoh 1:49
Yoh 12:13
l Mk 15:32
m Zb 3:2
Zb 22:8
Zb 42:10
n Mk 14:62
Yoh 5:18
Yoh 10:36
o Mk 15:32
Lu 23:39
p Amo 8:9
q Mk 15:33
Lu 23:44

35 Walipokuwa wamemtundika mtini[a] wakagawa mavazi yake ya nje[b] kwa kupiga kura,[c] **36** na, huku wakiwa wameketi, wakamlinda hapo. **37** Pia, wakabandika juu ya kichwa chake shtaka juu yake, kwa kuandika: "Huyu ni Yesu Mfalme wa Wayahudi."[d]

38 Ndipo wanyang'anyi wawili wakatundikwa mtini pamoja naye, mmoja upande wake wa kuume na mwingine upande wake wa kushoto.[e] **39** Kwa hiyo wapita-njia wakaanza kumtukana,[f] wakitikisa[g] vichwa vyao **40** na kusema: "Ewe uliyetaka kuliangusha hekalu[h] na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe mwenyewe! Ikiwa wewe ni mwana wa Mungu, shuka kutoka kwenye mti wa mateso!"[i] **41** Vivyo hivyo pia wakuu wa makuhani pamoja na waandishi na wanaume wazee wakaanza kumfanyia dhihaka na kusema:[j] **42** "Aliwaokoa wengine; yeye mwenyewe hawezi kujiokoa! Yeye ni Mfalme[k] wa Israeli; acheni sasa ashuke kutoka kwenye mti wa mateso nasi tutamwamini.[l] **43** Ameweka tegemeo lake katika Mungu; acheni Yeye sasa amwokoe[m] ikiwa Yeye anamtaka, kwa maana alisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu.'"[n] **44** Vivyo hivyo hata wanyang'anyi waliotundikwa mtini pamoja naye wakaanza kumshutumu.[o]

45 Tangu saa sita na kuendelea kukawa na giza[p] juu ya nchi yote, mpaka saa tisa.[q] **46** Karibu saa tisa Yesu akapaaza kilio kwa sauti kubwa, akisema: *"Eli, Eli, lama sabakthani?"*

yaani, "Mungu wangu, Mungu
wangu, kwa nini umeniacha?"[a]
47 Waliposikia hilo, baadhi ya
wale waliokuwa wamesima-
ma hapo wakaanza kusema:
"Mtu huyu anamwita Eliya."[b]
48 Na mmoja wao akakimbia
mara moja, akachukua sifongo
akailowesha kwenye divai kali[c]
akaiweka juu ya utete na ku-
anza kumnywesha.[d] **49** La-
kini wale wengine wao waka-
sema: "Acha iwe hivyo kwake!
Acheni tuone kama Eliya ata-
kuja kumwokoa."[e] [[Mtu mwi-
ngine akachukua mkuki na ku-
mchoma ubavuni, na damu na
maji vikatoka.]][f] **50** Tena
Yesu akapaaza sauti kubwa,
akaitoa roho yake.[g]

51 Na, tazama! pazia[h] la pa-
takatifu likapasuka vipande
viwili, kutoka juu mpaka chi-
ni,[i] na dunia ikatetemeka, na
miamba ikapasuka.[j] **52** Na
makaburi yakafunguka na mii-
li mingi ya watakatifu waliooku-
wa wamelala usingizi ikainuliwa,
53 (na watu, waliokuwa
wakitoka kati ya makaburi ba-
ada ya kufufuliwa kwake, wa-
kaingia katika jiji takatifu,)[k]
nayo ikaonwa na watu wengi.
54 Lakini yule ofisa-jeshi na
wale waliokuwa pamoja naye
wakimlinda Yesu, walipoona
tetemeko la nchi na mambo ya-
liyokuwa yakitendeka, wakao-
gopa sana, wakisema: "Hakika
huyu alikuwa Mwana wa Mu-
ngu."[l]

55 Zaidi ya hayo, wanawake
wengi walikuwa hapo wakita-
zama wakiwa mbali,[m] waliooku-
wa wamefuatana na Yesu kuto-
ka Galilaya ili kumhudumia;[n]
56 ambao kati yao alikuwa-
mo Maria Magdalene, pia Ma-
ria mama ya Yakobo na Yose,
na mama ya wana wa Zebe-
dayo.[a]

57 Sasa kwa kuwa ilikuwa
jioni, mtu mmoja tajiri wa
Arimathea, anayeitwa Yose-
fu, ambaye yeye mwenyewe
pia alikuwa mwanafunzi wa
Yesu, akaja.[b] **58** Mtu huyu
alimwendea Pilato na kuo-
mba apewe mwili wa Yesu.[c]
Ndipo Pilato akaamuru apewe
huo.[d] **59** Na Yosefu akauchu-
kua mwili huo, akaufunga ka-
tika kitani safi kizuri,[e] **60** na
kuulaza katika kaburi lake
jipya,[f] alilokuwa amechimba
katika mwamba. Na, baada
ya kuviringisha jiwe kubwa
kwenye mlango wa lile kaburi,
akaondoka.[g] **61** Lakini Ma-
ria Magdalene na yule Maria
mwingine wakabaki hapo, wa-
kiwa wameketi mbele ya kabu-
ri hilo.[h]

62 Siku iliyofuata, baada ya
yale Matayarisho,[i] wakuu wa
makuhani na Mafarisayo wali-
kusanyika pamoja mbele ya Pi-
lato, **63** wakisema: "Bwana,
tumekumbuka kwamba mja-
nja huyo alisema alipokuwa
bado yuko hai, 'Baada ya siku
tatu[j] nitafufuliwa.' **64** Kwa
hiyo amuru kaburi lilindwe
mpaka siku ya tatu, ili wanafu-
nzi wake wasipate kamwe kuja
na kumwiba[k] na kuwaambia
watu, 'Alifufuliwa kutoka kwa
wafu!' na ujanja huu wa mwi-
sho utakuwa mbaya zaidi kuli-
ko ule wa kwanza." **65** Pilato
akawaambia: "Ninyi mna wa-
linzi.[l] Nendeni mkalilinde jinsi
mnavyojua." **66** Basi wakae-
nda na kulilinda kaburi kwa

SURA 27
a Zb 22:1
Isa 53:10
Mk 15:34
b Mk 15:35
c Zb 69:21
d Lu 23:36
Yoh 19:29
e Mk 15:36
f Yoh 19:34
g Mk 15:37
Lu 23:46
Yoh 19:30
h Kut 26:31
Ebr 9:3
Ebr 10:20
i Mk 15:38
Lu 23:45
j 1Sa 14:15
k Mt 4:5
l Mk 15:39
Lu 23:47
m Lu 23:49
n Mk 15:41
Lu 8:3

Safu ya 2
a Mt 20:20
Mk 15:40
Yoh 19:25
b Mk 15:43
c Kum 21:23
Mk 15:43
Lu 23:52
d Mk 15:45
Yoh 19:38
e Mk 15:46
Lu 23:53
Yoh 19:40
f Isa 53:9
Mdo 13:29
g Mk 15:46
Lu 23:53
Yoh 19:41
h Mk 15:47
Lu 23:55
i Mk 15:42
Lu 23:54
Yoh 19:14
j Mt 12:40
Yoh 2:19
k Mt 28:13
l Mt 28:11

kulitia jiwe muhuri[a] na kuweka walinzi.

28 Baada ya siku ya sabato, kulipokuwa kukipambazuka katika siku ya kwanza ya juma, Maria Magdalene na yule Maria mwingine wakaja kulitazama kaburi.[b]
2 Na, tazama! tetemeko kubwa la nchi lilikuwa limetukia; kwa maana malaika wa Yehova alikuwa ameshuka kutoka mbinguni akakaribia na kuliviringisha jiwe, naye alikuwa ameketi juu yake.[c] **3** Alionekana kama umeme,[d] na mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji.[e] **4** Ndiyo, wale walinzi wakatetemeka na kuwa kama wafu kwa sababu ya kumwogopa.
5 Lakini malaika[f] akawajibu wanawake hao, akawaambia: "Msiogope, kwa maana ninajua mnamtafuta Yesu[g] aliyetundikwa mtini. **6** Hayupo hapa, kwa maana alifufuliwa,[h] kama alivyosema. Njooni, tazameni mahali alipokuwa amelala. **7** Nanyi nendeni upesi mkawaambie wanafunzi wake kwamba amefufuliwa[i] kutoka kwa wafu, na, tazama! atawatangulia kuingia Galilaya;[j] huko mtamwona. Tazama! Nimewaambia ninyi."[k]
8 Kwa hiyo, wakaondoka upesi kaburini, wakiwa na woga na shangwe kubwa, wakakimbia kuwajulisha wanafunzi wake.[l] **9** Na, tazama! Yesu akakutana nao na kusema: "Siku njema!" Wao wakakaribia, wakamshika miguu yake, wakamsujudia. **10** Ndipo Yesu akawaambia: "Msiogope! Nendeni, mkawajulishe ndugu zangu,[m] ili wapate kwenda zao Galilaya; na huko wataniona."
11 Walipokuwa wameondoka na kwenda, tazama! baadhi ya walinzi[a] wakaingia jijini na kuwaambia wakuu wa makuhani mambo yote yaliyokuwa yametukia. **12** Na walipokuwa wamekusanyika pamoja wakiwa na wanaume wazee na kushauriana, wakawapa hao askari-jeshi kiasi cha kutosha cha vipande vya fedha[b] **13** na kusema: "Semeni, 'Wanafunzi wake[c] walikuja wakati wa usiku wakamwiba tulipokuwa tumelala usingizi.' **14** Na hilo likifika masikioni mwa gavana, tutamshawishi na tutawaondolea ninyi wasiwasi." **15** Kwa hiyo wakachukua vile vipande vya fedha wakafanya kama walivyoagizwa; na maneno hayo yamesambazwa kotekote kati ya Wayahudi mpaka leo hii.
16 Hata hivyo, wale wanafunzi kumi na mmoja wakaingia Galilaya[d] mpaka kwenye mlima ambako Yesu alikuwa amewafanyia mpango, **17** nao walipomwona wakasujudu, lakini baadhi yao walikuwa na shaka.[e] **18** Naye Yesu akakaribia na kuwaambia, akisema: "Nimepewa mamlaka yote[f] mbinguni na duniani. **19** Kwa hiyo nendeni mkafanye wanafunzi[g] kutoka kwa watu wa mataifa yote,[h] mkiwabatiza[i] katika jina la Baba[j] na la Mwana[k] na la roho takatifu,[l] **20** na kuwafundisha[m] kushika[n] mambo yote ambayo nimewaamuru ninyi.[o] Na, tazama! mimi nipo pamoja nanyi[p] siku zote mpaka umalizio wa mfumo wa mambo."[q]

SURA 27
a Da 6:17

SURA 28
b Mk 16:1 Lu 24:1 Lu 24:10 Yoh 20:1
c Mk 16:4 Lu 24:2
d Amu 13:6 Da 10:6
e Mk 16:5 Lu 24:4 Mdo 1:10 Ufu 10:1
f Ebr 1:14
g Mk 16:6
h Mt 16:21 Mt 17:23 Lu 24:6 1Ko 15:4
i 2Ti 2:8
j Mt 26:32 Mt 28:16 Mk 14:28
k Mk 16:7
l Mk 16:8 Lu 24:9
m Yoh 20:17 Ro 8:29 Ebr 2:11

Safu ya 2
a Mt 27:65
b Met 17:23
c Mt 27:64
d Mt 26:32 1Ko 15:6
e Mt 14:31
f Da 7:14 Mt 11:27 Efe 1:21 Flp 2:9
g Mdo 14:21 Mdo 21:16
h Mdo 1:8 Ro 10:18 Ro 11:13 Ufu 14:6
i Mdo 2:38 Mdo 8:12
j Zb 83:18 Isa 64:8
k Flp 2:9 Ufu 19:16
l Yoh 14:16
m Mt 5:19 Mdo 20:20 2Ti 2:2
n Mt 7:24 Yoh 14:23 1Ti 6:14
o 1Ko 11:23 2Pe 3:2 1Yo 3:23
p Mt 18:20 Mdo 18:10
q Mt 13:39 Mt 13:49 Mt 24:3

KULINGANA NA

MARKO

1 Mwanzo wa habari njema juu ya Yesu Kristo:
2 Kama ilivyoandikwa katika
nabii Isaya: "(Tazama! Ninamtu-
ma mjumbe wangu mbele ya
uso wako, ambaye atakutaya-
rishia njia;)[a] **3** sikilizeni! mtu
fulani anapaaza sauti nyika-
ni, 'Tayarisheni njia ya Yeho-
va, nyoosheni barabara zake,'"[b]
4 Yohana mbatizaji alitokea
nyikani, akihubiri ubatizo unao-
onyesha toba ili kupata msama-
ha wa dhambi.[c] **5** Kwa saba-
bu hiyo eneo lote la Yudea na
wakaaji wote wa Yerusalemu
wakamwendea, naye akawaba-
tiza katika Mto Yordani, waki-
ungama waziwazi dhambi zao.[d]
6 Basi Yohana alikuwa amevaa
manyoya ya ngamia na mshi-
pi wa ngozi kiunoni mwake,[e]
na alikuwa akila nzige[f] na asali
ya mwituni.[g] **7** Naye alikuwa
akihubiri, akisema: "Baada ya-
ngu mtu fulani mwenye nguvu
kuliko mimi anakuja; mimi si-
stahili kuinama nizifungue ka-
mba za viatu vyake.[h] **8** Mimi
niliwabatiza ninyi kwa maji, la-
kini yeye atawabatiza ninyi kwa
roho takatifu."[i]

9 Baada ya siku hizo Yesu
akaja kutoka Nazareti ya Gali-
laya, Yohana akambatiza kati-
ka Yordani.[j] **10** Mara moja ali-
popanda kutoka majini akao-
na mbingu zikifunguka, na roho
ikashuka juu yake kama nji-
wa;[k] **11** na sauti ikaja kuto-
ka mbinguni: "Wewe ni Mwa-
nangu, mpendwa; nimekuku-
bali wewe."[l]

SURA 1

a Mal 3:1
Mt 11:10
Lu 7:27
b Isa 40:3
Lu 3:4
Yoh 1:23
c Mt 3:2
Lu 3:3
Mdo 13:24
d Met 28:13
Mal 3:5
Mdo 19:4
e 2Fa 1:8
f Law 11:22
g Mt 3:4
h Yoh 1:27
Mdo 13:25
i Isa 44:3
Yoe 2:28
Lu 3:16
Mdo 2:4
Mdo 11:16
1Ko 12:13
j Mt 3:13
k Isa 42:1
Mt 3:16
Lu 3:22
Yoh 1:32
l Zb 2:7
Mt 3:17
2Pe 1:17

Safu ya 2

a Lu 4:1
b Mt 4:2
c Mt 4:1
d Mt 4:11
e Mt 4:12
Lu 4:14
f Lu 8:1
g Da 9:26
Ga 4:4
Efe 1:10
h Mt 4:17
i Mt 10:2
j Mt 4:18
Lu 5:4
k Mt 4:19
l Mt 19:27
Lu 5:11
m Mt 4:21
n Mt 4:13
Lu 4:31
o Mt 7:28

12 Mara moja ile roho ika-
mshurutisha aende nyikani.[a]
13 Basi akakaa nyikani siku
40,[b] akijaribiwa na Shetani,[c]
naye alikuwa pamoja na wa-
nyama-mwitu, lakini malaika
walikuwa wakimhudumia.[d]

14 Basi baada ya Yohana ku-
kamatwa Yesu akaenda Galila-
ya,[e] akihubiri habari njema ya
Mungu[f] **15** na kusema: "Wa-
kati uliowekwa umetimizwa,[g]
na ufalme wa Mungu umekari-
bia. Tubuni,[h] na kuwa na ima-
ni katika habari njema."

16 Alipokuwa akitembea
kando ya bahari ya Galilaya
alimwona Simoni[i] na An-
drea ndugu ya Simoni wakitu-
pa nyavu zao huku na huku
katika bahari, kwa maana wa-
likuwa wavuvi.[j] **17** Kwa hiyo
Yesu akawaambia: "Nifuateni,
nami nitawafanya ninyi kuwa
wavuvi wa watu."[k] **18** Mara
moja wakaziacha nyavu zao na
kumfuata.[l] **19** Baada ya ku-
songa mbele kidogo akamwo-
na Yakobo mwana wa Zebeda-
yo na Yohana ndugu yake wali-
pokuwa katika mashua yao
wakitengeneza nyavu zao;[m]
20 na bila kukawia akawaita.
Nao wakamwacha baba yao Ze-
bedayo katika mashua hiyo pa-
moja na watu walioajiriwa, wa-
kamfuata. **21** Nao wakaenda
Kapernaumu.[n]

Mara baada ya hapo ilipo-
kuwa siku ya sabato akaingia
katika sinagogi akaanza ku-
fundisha. **22** Nao wakastaa-
jabia njia yake ya kufundisha,[o]

kwa maana huko alikuwa akiwafundisha kama mwenye mamlaka, na si kama waandishi.[a]
23 Pia, wakati uleule katika sinagogi lao kulikuwako na
mtu aliyekuwa chini ya nguvu
za roho mchafu, naye akapaaza sauti,[b] **24** akisema: "Tuna
nini nawe, Yesu Mnazareti?[c] Je,
umekuja kutuangamiza? Ninajua[d] wewe ni nani, Mtakatifu[e]
wa Mungu."[f] **25** Lakini Yesu
akamkemea, akisema: "Nyamaza, na umtoke!"[g] **26** Na
yule roho mchafu, baada ya kumfanya agaegae na kupiga kelele kwa sauti kubwa, akamtoka.[h] **27** Basi, watu wote wa-
kashangaa sana hivi kwamba
wakaanza mazungumzo kati
yao wenyewe, wakisema: "Ni
nini hili? Ni fundisho jipya!
Yeye anawaagiza kwa nguvu
zenye mamlaka hata roho wa-
chafu, nao humtii."[i] **28** Kwa
hiyo habari juu yake ikasambaa mara moja pande zote
za nchi yote inayozunguka Galilaya.[j]

29 Nao wakatoka mara
moja katika sinagogi wakaingia katika nyumba ya Simoni[k]
na Andrea pamoja na Yakobo
na Yohana. **30** Basi mama-
mkwe[l] wa Simoni alikuwa
amelala chini akiugua homa,[m]
nao mara moja wakamwambia Yesu juu yake. **31** Naye
akamwendea akamwinua, aka-
mshika mkono; na homa ika-
mwacha,[n] naye akaanza kuwa-
hudumia.[o]

32 Baada ya kuwa jioni, wa-
kati jua lilipokuwa limetua,
watu wakaanza kumletea watu
wote waliokuwa wagonjwa[p]
na waliokuwa na roho waovu;[q]
33 na jiji lote lilikuwa lime-
kusanyika palepale mlango-
ni. **34** Kwa hiyo akawapo-
nya wengi waliokuwa na ma-
gonjwa ya namna mbalimba-
li,[a] naye akafukuza roho waovu
wengi, lakini hakuwa akiwaru-
husu roho waovu waseme, kwa
sababu walijua kuwa yeye ni
Kristo.[b]

35 Na asubuhi na mapema,
kulipokuwa bado kuna giza,
akatoka nje akaenda maha-
li ambapo hapakuwa na watu,[c]
na huko akaanza kusali.[d]
36 Hata hivyo, Simoni na wale
waliokuwa pamoja naye waka-
mtafuta kwa bidii **37** na
kumpata, nao wakamwambia:
"Watu wote wanakutafuta."
38 Lakini akawaambia: "Twen-
deni mahali pengine, katika
miji ya vijiji iliyo karibu, ili ni-
pate kuhubiri huko pia,[e] kwa
maana nilitoka kwa kusudi
hilo."[f] **39** Naye akaenda, aki-
hubiri katika masinagogi yao
katika Galilaya yote na kufu-
kuza roho waovu.[g]

40 Huko pia mtu mwenye
ukoma akamjia, akimsihi hata
kwa kupiga magoti, akamwa-
mbia: "Ikiwa tu unataka, una-
weza kunitakasa."[h] **41** Ndi-
po akamsikitikia,[i] naye aka-
nyoosha mkono wake akamgu-
sa, akamwambia: "Ninataka.
Takasika."[j] **42** Na mara moja
ule ukoma ukamtoka, naye
akawa safi.[k] **43** Zaidi ya hilo,
akampa maagizo thabiti na
mara moja akamwacha aende,
44 na kumwambia: "Usimwa-
mbie mtu yeyote hata jambo
moja, bali nenda ujionyeshe
kwa kuhani[l] na kutoa vile vitu
alivyoamuru Musa kwa ajili ya
kutakaswa[m] kwako, ili kuwa

SURA 1
a Mt 7:29
b Lu 4:33
c Mt 8:29
d Yak 2:19
e Ufu 3:7
f Lu 4:34
g Lu 4:35
h Mk 9:20
Mk 9:26
i Lu 4:36
j Mt 4:24
Lu 4:37
k Lu 4:38
l 1Ko 9:5
m Mt 8:14
n Zb 103:3
o Mt 8:15
Lu 4:39
p Mt 4:24
Lu 4:40
q Mt 8:16

Safu ya 2
a Isa 53:4
b Mk 3:12
Lu 4:41
c Lu 4:42
d Mt 14:23
Mk 14:32
Ebr 5:7
e Isa 61:1
f Lu 4:43
Yoh 17:4
g Mt 4:23
Lu 4:44
h Mt 8:2
Lu 5:12
i Ebr 2:17
j Mt 8:3
k Lu 5:13
l Law 13:49
Law 14:3
m Law 14:10
Kum 24:8

ushahidi kwao."[a] **45** Lakini
baada ya kwenda zake mtu
huyo akaanza kutangaza sana
juu ya hilo na kusambaza ja-
mbo hilo kotekote, hivi kwa-
mba Yesu hakuweza tena kui-
ngia waziwazi katika jiji, lakini
akakaa nje katika mahali pasi-
po na watu. Na bado wakaende-
lea kumjia kutoka pande zote.[b]

2 Hata hivyo, baada ya siku
kadhaa akaingia tena Ka-
pernaumu na habari zikae-
nea kwamba yuko nyumbani.[c]
2 Kwa hiyo wengi wakakusa-
nyika, wengi sana hivi kwa-
mba hapakuwa na nafasi tena,
hata karibu na mlango, naye
akaanza kuwaambia lile neno.[d]
3 Na watu wakaja wakimle-
tea mtu mwenye kupooza aki-
wa amebebwa na watu wanne.[e]
4 Lakini kwa kutoweza ku-
mleta moja kwa moja mpaka
alipokuwa Yesu kwa sababu
ya umati, wakaiondoa paa juu
ya mahali alipokuwa, na baa-
da ya kutoboa tundu wakakite-
remsha kitanda ambacho juu
yake yule mwenye kupooza
alikuwa amelala.[f] **5** Na Yesu
alipoona imani[g] yao akamwa-
mbia yule mwenye kupooza:
"Mwanangu, dhambi zako zi-
mesamehewa."[h] **6** Basi hapo
palikuwa na baadhi ya wa-
andishi, wakiwa wameketi
na kuwaza mioyoni mwao:[i]
7 "Kwa nini mtu huyu ana-
ongea namna hii? Anakufu-
ru. Nani anayeweza kusamehe
dhambi ila mmoja, Mungu?"[j]
8 Lakini Yesu, baada ya kuta-
mbua mara moja rohoni mwa-
ke kwamba walikuwa waki-
waza hivyo ndani yao wenye-
we, akawaambia: "Kwa nini
mnawaza mambo haya mioyo-
ni mwenu?[a] **9** Ni jambo gani
lililo rahisi zaidi, kumwambia
mwenye kupooza, 'Umesame-
hewa dhambi zako,' au kuse-
ma, 'Simama, uchukue kitanda
chako, utembee'?[b] **10** Lakini
ili mjue kwamba Mwana wa
binadamu[c] ana mamlaka ya
kusamehe dhambi duniani,"[d]
—akamwambia yule mwenye
kupooza: **11** "Ninakuambia,
Simama, uchukue kitanda cha-
ko, uende nyumbani kwako."[e]
12 Ndipo akaondoka, akachu-
kua mara moja kitanda chake,
akatembea mbele yao wote na
kwenda nje,[f] hivi kwamba wote
wakastaajabu, nao wakamtu-
kuza Mungu, wakisema: "Ha-
tujaona kamwe jambo kama
hilo."[g]

13 Tena akaenda kando ya
bahari; na umati wote uka-
endelea kumjia, naye akaa-
nza kuufundisha. **14** Lakini
alipokuwa akipita kandoka-
ndo, akamwona Lawi[h] mwana
wa Alfayo akiwa ameketi kwe-
nye ofisi ya kodi, naye akamwa-
mbia: "Uwe mfuasi wangu."
Naye akaondoka, akamfua-
ta.[i] **15** Baadaye akawa ame-
keti mezani, nyumbani kwa-
ke, na wakusanya-kodi[j] we-
ngi na watenda-dhambi walikuwa
wameketi pamoja na Yesu
na wanafunzi wake, kwa maa-
na walikuwa wengi nao waka-
anza kumfuata.[k] **16** Lakini
waandishi wa Mafarisayo, wa-
lipoona alikuwa akila pamo-
ja na watenda-dhambi na wa-
kusanya-kodi, wakaanza ku-
waambia wanafunzi wake: "Je,
yeye hula pamoja na wakusa-
nya-kodi na watenda-dhambi?"[l]

SURA 1

a Mt 8:4
Lu 5:14

b Mk 2:13
Lu 5:15

SURA 2

c Mt 9:1

d Zb 40:9
Isa 61:1
Efe 2:17
Ebr 2:3

e Mt 9:2
Lu 5:18

f Lu 5:19

g Mdo 14:9

h Isa 53:11
Lu 5:20
Lu 7:48

i Lu 5:21

j Zb 130:4
Isa 43:25

Safu ya 2

a Zb 7:9
Mt 9:4
Lu 6:8
Ebr 4:13
Ufu 2:23

b Mt 9:5
Lu 5:23

c Da 7:13

d Isa 53:11
Mdo 5:31

e Mt 9:6
Lu 5:24

f Mt 9:8
Lu 5:26

g Mt 9:33
Yoh 7:31
Yoh 9:32

h Mt 9:9

i Lu 5:27

j Lu 15:1

k Mt 9:10
Lu 5:29

l Isa 65:5
Mt 9:11
Lu 5:31

17 Aliposikia hilo Yesu akawa-
ambia: "Wale walio na nguvu
hawahitaji tabibu, bali wale wa-
lio wagonjwa wanamhitaji. Ni-
likuja kuwaita, si watu waadili-
fu, bali watenda-dhambi."[a]

18 Basi wanafunzi wa Yoha-
na na Mafarisayo walikuwa na
zoea la kufunga. Kwa hiyo wa-
kaja wakamwambia: "Kwa nini
wanafunzi wa Yohana na wa-
nafunzi wa Mafarisayo hufu-
nga, lakini wanafunzi wako ha-
wafungi?"[b] **19** Na Yesu aka-
waambia: "Je, wakati bwana-
arusi yupo pamoja nao rafiki
za bwana-arusi wanaweza ku-
funga?[c] Maadamu wana bwa-
na-arusi pamoja nao hawawezi
kufunga.[d] **20** Lakini siku zi-
takuja wakati ambapo bwana-
arusi ataondolewa kwao, ndi-
po watakapofunga siku hiyo.[e]
21 Hakuna mtu anayeshona
kiraka cha nguo mpya juu ya
vazi la nje la zamani; akifa-
nya hivyo, nguvu zake huvu-
ta ile nguo mpya kutoka kwe-
nye lile vazi la zamani, nalo
huraruka vibaya zaidi.[f] **22** Pia,
hakuna mtu anayeweka divai
mpya ndani ya viriba vya divai
vilivyozeeka; akifanya hivyo,
divai hupasua ngozi ya viriba
hivyo, na divai hupotea na vi-
levile ngozi.[g] Bali watu huweka
divai mpya ndani ya viriba vi-
pya vya divai."[h]

23 Basi akawa akipita kati-
kati ya mashamba ya nafa-
ka siku ya sabato, na wana-
funzi wake wakaanza kupi-
ta waking'oa[i] masuke ya nafa-
ka.[j] **24** Kwa hiyo Mafarisayo
wakaanza kumwambia: "Ta-
zama sasa! Kwa nini wana-
fanya jambo lisilo halali kati-
ka siku ya sabato?"[k] **25** La-
kini yeye akawaambia: "Je,
hamjasoma hata mara moja ja-
mbo alilofanya Daudi[a] alipo-
kuwa na uhitaji akaona njaa,
yeye na wale watu waliokuwa
pamoja naye?[b] **26** Jinsi ali-
vyoingia ndani ya nyumba ya
Mungu, katika lile simulizi juu
ya Abiathari[c] mkuu wa maku-
hani, akala mikate ya toleo,[d]
ambayo si halali[e] kwa mtu ye-
yote kula ila makuhani, naye
akawapa wale watu waliokuwa
pamoja naye sehemu yake
pia?"[f] **27** Kwa hiyo akaende-
lea kuwaambia: "Sabato ilikuja
kwa ajili ya mwanadamu,[g]
wala si mwanadamu kwa aji-
li ya sabato;[h] **28** kwa sababu
hiyo Mwana wa binadamu ni
Bwana hata wa sabato."[i]

3 Mara nyingine tena akai-
ngia katika sinagogi, na
mtu mmoja mwenye mko-
no uliopooza alikuwa humo.[j]
2 Kwa hiyo walikuwa waki-
mchunguza sana waone kama
angemponya mtu huyo kati-
ka siku ya sabato, ili wapa-
te kumshtaki.[k] **3** Naye aka-
mwambia mtu huyo mwenye
mkono uliopooza: "Simama uje
katikati." **4** Halafu akawa-
ambia: "Je, katika siku ya sa-
bato ni halali kutenda tendo
jema au kutenda tendo baya,
kuokoa au kuua nafsi?"[l] Laki-
ni wao wakakaa kimya. **5** Na
baada ya kuwatazama huku
na huku kwa ghadhabu, akiwa
amehuzunishwa na jinsi mioyo
yao[m] ilivyokuwa migumu, aka-
mwambia mtu huyo: "Nyoosha
mkono wako." Naye akaunyoo-
sha, na mkono wake ukapona.[n]
6 Ndipo Mafarisayo wakatoka
na mara moja wakaanza kufa-

SURA 2
a Isa 61:1
Mt 9:12
Lu 5:31
Lu 19:10
1Ti 1:15
b Mt 9:14
Lu 5:33
c Yoh 3:29
d Zb 45:Uta-17
Mt 22:2
2Ko 11:2
Ufu 19:7
e Mt 9:15
Lu 5:35
Lu 17:22
f Mt 9:16
Lu 5:36
g Ayu 32:19
h Mt 9:17
Lu 5:38
i Kum 23:25
j Mt 12:1
Lu 6:1
k Mt 12:2

Safu ya 2
a 1Sa 21:6
b Mt 12:3
Lu 6:3
c 1Sa 22:20
d Law 24:6
e Kut 25:30
Kut 29:32
Law 24:9
f Lu 6:4
g Kut 20:10
Eze 20:12
h Mt 12:7
Kol 2:16
i Mt 12:8
Lu 6:5

SURA 3
j Mt 12:9
Lu 6:6
k Mt 12:10
Lu 6:7
Lu 14:1
l Mt 12:11
Lu 14:3
m Yoh 12:40
Ro 11:25
n Mt 12:13
Lu 6:10

nya baraza pamoja na wafuasi wa chama cha Herode[a] juu yake, ili wamwangamize.[b]

7 Lakini Yesu pamoja na wanafunzi wake wakaondoka kwenda baharini; na umati mkubwa kutoka Galilaya na kutoka Yudea ukamfuata.[c] **8** Hata kutoka Yerusalemu na kutoka Idumea na kutoka ng'ambo ya Yordani na kuzunguka Tiro[d] na Sidoni, umati mkubwa, uliposikia alikuwa akifanya mambo mengi, ukamjia. **9** Naye akawaambia wanafunzi wake wawe na mashua ndogo sikuzote ya kutumia ili umati usiweze kumsonga. **10** Kwa kuwa aliwaponya watu wengi, wale wote waliokuwa na magonjwa yenye kuhuzunisha walikuwa wakimwangukia ili wamguse.[e] **11** Hata roho wachafu,[f] walipokuwa wakimwona, walikuwa wakijiangusha wenyewe chini mbele yake na kupaaza sauti, wakisema: "Wewe ndiye Mwana wa Mungu."[g] **12** Lakini mara nyingi aliwaagiza kwa kusisitiza wasifanye ajulikane.[h]

13 Naye akapanda mlima na kuwaita wale aliotaka,[i] nao wakamwendea.[j] **14** Naye akafanyiza kikundi cha watu kumi na wawili, ambao pia aliwaita "mitume," ili waendelee kuwa pamoja naye na awatume wakahubiri[k] **15** na kuwa na mamlaka ya kuwafukuza roho waovu.[l]

16 Na kikundi cha wale kumi na wawili aliofanyiza walikuwa Simoni, ambaye pia alimpa jina Petro,[m] **17** na Yakobo mwana wa Zebedayo na Yohana ndugu ya Yakobo[a] (hawa pia aliwapa jina Boanerge, ambalo linamaanisha Wana wa Ngurumo), **18** na Andrea na Filipo na Bartholomayo na Mathayo na Tomasi na Yakobo mwana wa Alfayo na Thadayo na Simoni Mkananayo **19** na Yuda Iskariote, ambaye baadaye alimsaliti.[b]

Naye akaingia ndani ya nyumba. **20** Mara nyingine tena umati ukakusanyika, hivi kwamba hawakuweza hata kula mlo.[c] **21** Lakini watu wa jamaa[d] yake waliposikia juu ya hilo, wakatoka kwenda kumshika, kwa maana walikuwa wakisema: "Amerukwa na akili."[e] **22** Pia, waandishi walioteremka kutoka Yerusalemu walikuwa wakisema: "Ana Beelzebuli, naye huwafukuza roho waovu kwa njia ya mtawala wa roho waovu."[f] **23** Kwa hiyo, baada ya kuwaita, akaanza kuzungumza nao kwa mifano: "Shetani anawezaje kumfukuza Shetani? **24** Kwani, ufalme ukigawanyika dhidi yake wenyewe, ufalme huo hauwezi kusimama;[g] **25** na nyumba ikigawanyika dhidi yake yenyewe, nyumba hiyo haitaweza kusimama.[h] **26** Pia, ikiwa Shetani ameinuka dhidi yake mwenyewe na kugawanyika, hawezi kusimama, bali anafikia mwisho.[i] **27** Kwa kweli, hakuna yeyote ambaye ameingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu anayeweza kupora[j] mali zake zinazoweza kuchukuliwa asipomfunga kwanza mtu huyo mwenye nguvu, na ndipo ataipora nyumba yake.[k] **28** Kwa kweli ninawaambia

SURA 3
a Mt 22:16 Mk 12:13
b Mt 12:14 Lu 6:11 Yoh 11:53
c Mt 12:15 Lu 6:17
d Mt 11:21
e Mt 9:21 Mk 5:28 Mk 6:56
f Mt 8:31 Mk 1:23
g Mk 5:7 Lu 4:41
h Mt 12:16 Mk 1:25
i Yoh 15:16
j Lu 6:12 Lu 9:1
k Lu 6:13
l Mt 10:1
m Yoh 1:42

Safu ya 2
a Mt 10:2 Lu 6:14 Lu 9:54 Mdo 1:13
b Mt 10:4 Lu 6:16
c Mk 6:31
d Yoh 7:5
e Yoh 10:20
f Mt 9:34 Mt 10:25 Lu 11:15 Yoh 8:48
g Mt 12:25
h Lu 11:17
i Mt 12:26 Lu 11:18
j Isa 49:24
k Mt 12:29

ninyi kwamba wana wa binadamu watasamehewa mambo yote, hata ziwe ni dhambi gani na makufuru wanayofanya kwa kukufuru.[a] **29** Hata hivyo, yeyote yule anayekufuru roho takatifu hatapata msamaha milele, bali ana hatia ya dhambi ya milele."[b] **30** Alisema hivyo kwa sababu walikuwa wakisema: "Ana roho mchafu."[c]

31 Sasa mama yake na ndugu zake[d] wakaja, na, walipokuwa wamesimama nje, wakatuma aitwe.[e] **32** Ikawa kwamba, umati ulikuwa umeketi kumzunguka, kwa hiyo wakamwambia: "Tazama! Mama yako na ndugu zako wako nje wanakutafuta."[f] **33** Lakini akajibu, akawaambia: "Mama yangu na ndugu zangu ni nani?"[g] **34** Na akiisha kuwatazama huku na huku wale waliokuwa wameketi kumzunguka, akasema: "Tazama, mama yangu na ndugu zangu![h] **35** Yeyote yule anayefanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu na dada yangu na mama yangu."[i]

4 Naye akaanza tena kufundisha kando ya bahari.[j] Na umati mkubwa sana ukakusanyika karibu naye, hivi kwamba akapanda ndani ya mashua akaketi baharini, lakini umati wote kando ya bahari ulikuwa pwani.[k] **2** Kwa hiyo akaanza kuwafundisha mambo mengi kwa mifano[l] na kuwaambia katika kufundisha kwake:[m] **3** "Sikilizeni. Tazama! Mpandaji alienda kupanda.[n] **4** Naye alipokuwa akipanda, mbegu fulani zikaanguka kando ya barabara, na ndege wakaja wakazila.[a] **5** Na mbegu nyingine zikaanguka mahali penye miamba ambapo, bila shaka, hapakuwa na udongo mwingi, nazo zikachipuka mara moja kwa sababu ya kutokuwa na udongo wenye kina.[b] **6** Lakini jua lilipochomoza, zikaungua, na kwa sababu hazikuwa na mzizi zikanyauka.[c] **7** Na mbegu nyingine zikaanguka katikati ya miiba, na ile miiba ikamea na kuzisonga, nazo hazikuzaa tunda lolote.[d] **8** Lakini nyingine zikaanguka kwenye udongo mzuri,[e] nazo zikamea na kuongezeka, zikaanza kuzaa matunda, nazo zilikuwa zikizaa matunda 30, na 60 na 100."[f] **9** Kwa hiyo akaongeza neno hili: "Yule aliye na masikio ya kusikiliza, na asikilize."[g]

10 Basi alipokuwa peke yake, wale waliomzunguka pamoja na wale kumi na wawili wakaanza kumuuliza juu ya mifano hiyo.[h] **11** Naye akaanza kuwaambia: "Ninyi mmepewa siri takatifu[i] ya ufalme wa Mungu, lakini kwa wale walio nje mambo yote yanatukia kwa mifano,[j] **12** ili, ingawa wanatazama, watazame na bado wasione, na, ingawa wanasikia, wasikie na bado wasielewe, wala wasigeuke kamwe na kusamehewa."[k] **13** Tena akawaambia: "Hamjui mfano huo, kwa hiyo basi mtaelewa namna gani mifano mingine yote?

14 "Mpandaji hulipanda neno.[l] **15** Basi, hawa ndio wale walio kando ya barabara ambapo lile neno limepandwa,

SURA 3
a Mt 12:31
Lu 12:10
b Mt 12:32
Ebr 6:4
Ebr 6:6
Ebr 10:26
1Yo 5:16
c Yoh 7:20
Yoh 10:20
d Mt 13:55
Yoh 2:12
Mdo 1:14
e Mt 12:46
Lu 8:19
f Mt 12:47
Mk 6:3
Lu 8:20
g Mt 10:37
h Mt 12:49
Ro 8:29
Ebr 2:11
i Mt 12:50
Lu 8:21
Yoh 15:14

SURA 4
j Isa 9:1
k Mt 13:1
Lu 8:4
l Mt 13:34
m Mt 13:3
Mk 12:38
n Mk 4:14
Lu 8:5

Safu ya 2
a Mt 13:4
b Mt 13:5
Mk 4:16
Mk 4:17
Lu 8:6
c Mt 13:6
Yak 1:11
d Mt 13:7
Mk 4:18
Mk 4:19
Lu 8:7
e Ebr 6:7
f Mt 13:8
Mk 4:20
Lu 8:8
Yoh 15:5
Kol 1:6
g Met 1:5
Mt 11:15
h Met 4:7
Mt 13:10
Lu 8:9
i Efe 1:9
Kol 1:26
j Mt 13:11
Lu 8:10
Kol 4:5
1Ti 3:7
k Kum 29:4
Isa 6:9
Yer 5:21
Mt 13:14
Yoh 12:40
Mdo 28:26
l Mt 13:19
1Pe 1:25

lakini mara tu baada ya kulisikia Shetani huja[a] na kuliondoa neno lililopandwa ndani yao.[b] **16** Vivyo hivyo hawa ndio wale waliopandwa mahali penye miamba: mara tu baada ya kulisikia neno, wanalipokea kwa shangwe.[c] **17** Lakini hawana mzizi ndani yao wenyewe, bali wao huendelea kuwako kwa wakati fulani; kisha mara tu dhiki au mateso yanapotokea kwa sababu ya lile neno, wao hukwazika.[d] **18** Bado kuna wengine wanaopandwa katikati ya miiba; hawa ndio ambao wamelisikia neno,[e] **19** lakini mahangaiko[f] ya mfumo huu wa mambo na nguvu za udanganyifu za utajiri[g] na tamaa[h] za mambo yale mengine hupenya na kulisonga neno, nalo hukosa kuzaa matunda.[i] **20** Mwishowe, wale waliopandwa kwenye udongo mzuri ndio wale wanaolisikiliza neno na kulipokea vizuri na kuzaa matunda mara 30 na 60 na 100."[j]

21 Naye akaendelea kuwaambia: "Je, taa huletwa ili kuwekwa chini ya kikapu cha kupimia au chini ya kitanda? Je, hailetwi ili kuwekwa juu ya kinara cha taa?[k] **22** Kwa maana hakuna jambo lililofichwa ila kwa kusudi la kupata kufunuliwa; hakuna lililositiriwa kwa uangalifu ila kwa kusudi la kuja kutokea wazi.[l] **23** Yeyote aliye na masikio ya kusikiliza, na asikilize."[m]

24 Tena akawaambia: "Sikilizeni kwa makini mambo ambayo mnasikia.[n] Kwa kipimo mnachopimia, mtapimiwa hicho,[o] ndiyo, mtaongezewa zaidi.[a] **25** Kwa maana aliye na kitu ataongezewa; lakini yule ambaye hana kitu, hata kile alicho nacho kitachukuliwa."[b]

26 Kwa hiyo akaendelea kusema: "Katika njia hii ufalme wa Mungu ni kama vile mtu anapotupa mbegu kwenye udongo,[c] **27** naye hulala usingizi usiku na huamka mchana, na ile mbegu huota na hukua na kuwa ndefu, naye hajui ni jinsi gani hasa.[d] **28** Udongo wenyewe hutokeza matunda hatua kwa hatua, kwanza jani, kisha suke, mwishowe nafaka iliyo kamili katika suke. **29** Lakini mara tu matunda yanaporuhusu, yeye huutia mundu, kwa sababu wakati wa mavuno umefika."

30 Naye akaendelea kusema: "Tutaufananisha ufalme wa Mungu na nini, au tutauweka katika mfano gani?[e] **31** Kama mbegu ya haradali, ambayo ilipopandwa katika udongo ilikuwa ndiyo mbegu ndogo zaidi kuliko zote duniani[f]— **32** lakini baada ya kupandwa, humea na kuwa kubwa zaidi kuliko mboga nyingine zote na hutokeza matawi makubwa,[g] hivi kwamba ndege wa mbinguni[h] wanaweza kupata makao chini ya kivuli chake."[i]

33 Kwa hiyo alikuwa akisema nao lile neno kwa mifano[j] mingi ya namna hiyo, kwa kadiri walivyoweza kusikiliza. **34** Kwa kweli, hakuwa akisema nao bila mfano, lakini kwa faragha alikuwa akiwaeleza wanafunzi wake mambo yote.[k]

SURA 4

a 2Ko 2:11; 1Pe 5:8
b Ebr 2:1
c Mt 13:20; Lu 8:13
d Mt 13:21
e Mt 13:22; Lu 8:14
f Mt 6:25; Mt 24:38
g Met 23:5; Mk 10:23; Lu 18:24; 1Ti 6:9; 2Ti 4:10
h 1Yo 2:16
i Mt 13:22; Lu 8:14
j Mt 13:23; Ro 7:4; Kol 1:10; 2Pe 1:8
k Mt 5:15; Lu 11:33
l Mt 10:26; Lu 12:2; Mdo 4:20; 1Ti 5:25; 1Yo 1:2
m Met 1:5; Mt 11:15; Ufu 2:7
n Lu 8:18; Yak 1:25
o Met 11:25

Safu ya 2

a Mt 7:2; Lu 6:38; 2Ko 9:6
b Mt 13:12; Mt 25:23; Lu 8:18; Lu 19:26
c Mt 13:24
d Mwa 1:11; Ga 6:7
e Mt 13:31; Lu 13:18
f Mt 13:32; Lu 13:19
g Da 4:12; Da 4:21
h Zb 104:12; Eze 31:6
i Mt 13:34
j Zb 78:2
k Mt 13:11; Mt 13:35; Mk 4:11

35 Na siku hiyo, ilipokuwa jioni, akawaambia: "Na tuvuke mpaka ukingo ule mwingine wa bahari."[a] **36** Kwa hiyo, walipokuwa wamekwisha kuuruhusu umati uondoke, wakamchukua katika mashua, kama vile alivyokuwa, na kulikuwa na mashua nyinginezo pamoja naye.[b] **37** Sasa kukatokea dhoruba kubwa ya upepo wenye nguvu nyingi, na mawimbi yakawa yakiipiga mashua kwa nguvu, hivi kwamba karibu mashua ifunikwe na maji.[c] **38** Lakini yeye alikuwa katika tezi, akiwa amelalia mto. Kwa hiyo wakamwamsha na kumwambia: "Mwalimu, je, hujali kwamba tuko karibu kuangamia?"[d] **39** Ndipo akaamka, akaukemea upepo na kuiambia bahari: "Nyamaza, utulie!"[e] Na upepo ukapunguka, kukawa utulivu mkubwa.[f] **40** Kwa hiyo akawaambia: "Kwa nini mna moyo wa woga? Je, bado hamna imani yoyote?" **41** Lakini wakaogopa isivyo kawaida, nao wakawa wakiambiana: "Kwa kweli huyu ni nani, kwa sababu hata upepo na bahari zinamtii?"[g]

5 Basi, wakafika upande ule mwingine wa bahari na kuingia katika nchi ya Wagerasene.[h] **2** Na mara tu alipotoka katika mashua mtu mmoja mwenye roho mchafu akakutana naye kutoka kati ya makaburi.[i] **3** Alikuwa akikaa katikati ya makaburi; na kufikia wakati huo hakuna mtu aliyeweza kumfunga hata kwa mnyororo, **4** kwa sababu alikuwa amefungwa mara nyingi kwa pingu na minyororo, lakini akaikata minyororo na kuzivunja pingu; wala hakuna mtu aliyekuwa na nguvu za kumshinda. **5** Na sikuzote, usiku na mchana alikuwa akipaaza sauti makaburini na milimani na kujikatakata kwa mawe. **6** Lakini alipomwona Yesu akiwa mbali akakimbia akamsujudia, **7** na, alipopaaza sauti kubwa,[a] akasema: "Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu Aliye Juu Zaidi?[b] Ninakuapisha[c] kwa Mungu usinitese."[d] **8** Kwa maana alikuwa amemwambia: "Mtoke mtu huyu, wewe roho mchafu."[e] **9** Lakini Yesu akaanza kumuuliza: "Jina lako ni nani?" Naye akamwambia: "Jina langu ni Kikosi,[f] kwa sababu tuko wengi."[g] **10** Naye akamsihi mara nyingi asiwafukuze roho hao watoke katika nchi hiyo.[h]

11 Basi kulikuwa na kundi kubwa la nguruwe[i] likilisha mlimani.[j] **12** Kwa hiyo wakamsihi, wakisema: "Acha twende kwa wale nguruwe, ili tuingie ndani yao." **13** Naye akawaruhusu. Ndipo wale roho wachafu wakatoka na kuingia ndani ya wale nguruwe; na lile kundi likatimua mbio, likaruka poromoko, likaingia baharini, wakiwa karibu elfu mbili, nao wakafa maji mmoja baada ya mwingine katika bahari.[k] **14** Lakini wachungaji wa nguruwe hao wakakimbia wakapeleka habari jijini na mashambani; na watu wakaja kuona kilichokuwa kimetukia.[l] **15** Kwa hiyo wakamjia Yesu, nao wakamwona yule mtu aliyekuwa na roho waovu akiwa ameketi amevaa nguo na akiwa na akili yake timamu, mtu

SURA 4
a Mt 8:18
b Mt 8:23 Lu 8:22
c Mt 8:24 Lu 8:23
d Mt 8:25 Lu 8:24
e Zb 89:9
f Mt 8:26 Lu 8:24
g Mt 8:27 Lu 8:25 Yoh 6:19

SURA 5
h Mt 8:28 Lu 8:26
i Lu 8:27

Safu ya 2
a Mdo 16:17
b 1Fa 17:18 Yak 2:19
c Mt 26:63
d Mt 8:29
e Mdo 16:18
f Mt 12:45
g Lu 8:30
h Lu 8:31
i Law 11:7 Kum 14:8
j Mt 8:30 Lu 8:32
k Mt 8:32 Lu 8:33
l Mt 8:33 Lu 8:35

yule aliyekuwa na kile kikosi;
nao wakaogopa. **16** Pia, wale
waliokuwa wameona jambo
hilo wakawasimulia jinsi ilivyo-
kuwa imetukia kwa mtu huyo
aliyekuwa na roho waovu na
juu ya wale nguruwe. **17** Na
kwa hiyo wakaanza kumsihi
atoke katika wilaya zao.[a]

18 Basi alipokuwa akipanda
mashua, yule mtu aliyekuwa
na roho waovu akaanza kumsi-
hi akae pamoja naye.[b] **19** Hata
hivyo, hakumruhusu, bali ali-
mwambia: "Nenda nyumbani
kwa watu wa jamaa yako,[c] uka-
waambie mambo yote amba-
yo Yehova[d] amekufanyia na ji-
nsi alivyokuonyesha rehema."[e]
20 Naye akaenda zake akaa-
nza kutangaza katika Dekapoli[f]
juu ya mambo yote ambayo Yesu
alimfanyia, na watu wote waka-
anza kustaajabu.[g]

21 Baada ya Yesu kuvuka
tena katika mashua na kuru-
di mpaka ule ukingo wa ba-
hari wa upande wa pili uma-
ti mkubwa ukakusanyika pa-
moja mahali alipokuwa; naye
alikuwa kando ya bahari.[h]
22 Sasa mmoja wa maofisa-
wasimamizi wa sinagogi, ana-
yeitwa Yairo, akaja na, alipo-
mwona, akamwangukia migu-
uni[i] **23** akamsihi mara nyi-
ngi, akisema: "Binti yangu
mdogo yuko katika hali mba-
ya sana. Njoo tafadhali uweke
mikono[j] yako juu yake ili apo-
ne na kuishi."[k] **24** Ndipo aka-
enda pamoja naye. Nao umati
mkubwa ulikuwa ukimfuata na
kumsonga.[l]

25 Basi kulikuwa na mwa-
namke aliyekuwa na mtiriri-
ko wa damu[m] kwa miaka kumi
na miwili,[a] **26** naye alikuwa
ameumizwa sana na matabibu
wengi[b] na alikuwa ametumia
mali zake zote naye hakuwa
amefaidika bali, badala yake,
hali yake ikawa mbaya zaidi.
27 Aliposikia juu ya Yesu, aka-
ja kutoka nyuma katika ule
umati na kuligusa[c] vazi lake
la nje; **28** kwa maana aliku-
wa akisema: "Nikiyagusa tu
mavazi yake ya nje nitapona."[d]
29 Na mara moja chemchemi
yake ya damu ikakauka, naye
akahisi mwilini mwake kwa-
mba alikuwa amepona ule ugo-
njwa wenye kuhuzunisha.[e]

30 Mara moja, pia, Yesu aka-
tambua ndani yake mwenyewe
kwamba nguvu[f] zilikuwa zime-
mtoka, naye akageuka huku na
huku katika ule umati na ku-
anza kusema: "Ni nani aliye-
yagusa mavazi yangu ya nje?"[g]
31 Lakini wanafunzi wake wa-
kaanza kumwambia: "Unaona
umati unavyokusonga,[h] nawe
unasema, 'Ni nani aliyenigu-
sa?'" **32** Hata hivyo, alikuwa
akitazama huku na huku ili
amwone mwanamke aliyeku-
wa amefanya hivyo. **33** Laki-
ni huyo mwanamke, akiogopa
na kutetemeka, akijua lililoku-
wa limetukia, akaja, akaangu-
ka chini mbele yake, akamwa-
mbia kweli yote.[i] **34** Yesu
akamwambia: "Binti yangu,
imani yako imekuponya. Ne-
nda kwa amani,[j] na uwe na afya
njema kutokana na ugonjwa
wako wenye kuhuzunisha."[k]

35 Alipokuwa bado akise-
ma, watu fulani kutoka nyu-
mbani kwa yule ofisa-msima-
mizi wa sinagogi wakaja na
kusema: "Binti yako amekufa!

SURA 5

a Mt 8:34
Lu 8:37
Mdo 16:39
1Ko 2:14

b Lu 8:38

c Mk 6:4

d Kut 18:8

e Ro 9:15
Efe 2:4

f Mk 7:31

g Lu 8:39

h Lu 8:40

i Lu 8:41

j Mk 6:5
Lu 4:40
Mdo 9:17

k Mt 9:18

l Mt 9:19
Lu 8:42

m Law 15:25

Safu ya 2

a Mt 9:20
Lu 8:43

b Zb 108:12

c Mt 14:36
Mk 6:56

d Law 6:27
Mt 9:21

e Lu 8:44

f Lu 5:17
Lu 6:19

g Lu 8:46

h Lu 8:45

i Lu 8:47

j Amu 18:6
1Sa 1:17
Lu 7:50
Lu 8:48

k Mt 9:22

Kwa nini uendelee kumsumbua
mwalimu?"[a] **36** Lakini Yesu
akasikia yaliyokuwa yakisemwa, akamwambia ofisa-msimamizi wa sinagogi: "Usiogope, uwe tu na imani."[b] **37** Basi
hakumruhusu mtu yeyote afuatane naye ila Petro na Yakobo
na Yohana ndugu ya Yakobo.[c]

38 Kwa hiyo wakafika kwenye nyumba ya yule ofisa-msimamizi wa sinagogi, naye akaona ule mvurugo wenye kelele
na wale wenye kulia na kupiga kelele nyingi za kuomboleza, **39** na, baada ya kuingia, akawaambia: "Kwa nini
mnatokeza mvurugo wenye kelele na kulia? Mtoto mchanga hakufa, bali analala usingizi."[d] **40** Ndipo wakaanza
kumcheka kwa dharau. Lakini, akiisha kuwatoa nje wote,
akamchukua baba na mama ya huyo mtoto mchanga na
walio pamoja naye, naye akaingia mahali alipokuwa mtoto
huyo.[e] **41** Na, akiushika mkono wa mtoto huyo, akamwambia: *"Talitha kumi,"* maneno
ambayo yanapotafsiriwa, yanamaanisha: "Mwanamwali, ninakuambia, Simama!"[f] **42** Na
mara yule mwanamwali akasimama akaanza kutembea,
kwa maana alikuwa na umri wa miaka kumi na miwili.
Na mara moja wakawa na shangwe kubwa.[g] **43** Lakini
akawaagiza tena na tena wasimwambie mtu yeyote[h] juu ya
hilo, naye akasema kwamba mtoto huyo apewe chakula ale.

6 Naye akatoka huko na kuingia katika eneo lake la nyumbani, na wanafunzi wake wa-
kamfuata.[i] **2** Ilipofika siku ya
sabato, akaanza kufundisha katika sinagogi; na hesabu kubwa zaidi ya wale waliokuwa wakisikiliza wakastaajabu
na kusema: "Mtu huyu alipata wapi mambo haya?[a] Na kwa
nini mtu huyu apewe hekima
hii, naye afanye matendo yenye nguvu hivyo kwa mikono
yake? **3** Je, huyu si yule seremala[b] mwana wa Maria[c] na
ndugu ya Yakobo[d] na Yosefu
na Yuda na Simoni?[e] Na dada
zake wapo hapa pamoja nasi,
sivyo?" Kwa hiyo wakaanza
kukwazika kwa sababu yake.[f]
4 Lakini Yesu akaendelea kuwaambia: "Nabii hakosi kuheshimiwa ila katika eneo lake
la nyumbani[g] na katikati ya
watu wa jamaa yake na katika nyumba yake mwenyewe."[h] **5** Kwa hiyo hakuweza
kufanya matendo yenye nguvu huko ila kuweka mikono
yake juu ya wagonjwa wachache na kuwaponya. **6** Kwa
kweli, alistaajabia ukosefu wao
wa imani. Naye akaenda akizunguka vijijini, akifundisha.[i]

7 Sasa akawaita wale kumi
na wawili, akaanza kuwatuma wawili-wawili,[j] naye akaanza kuwapa mamlaka juu ya
roho wachafu.[k] **8** Pia, akawaagiza wasichukue kitu chochote kwa ajili ya safari, wala
mkate, wala mfuko wa chakula,[l] wala pesa za shaba katika mikoba kwenye mishipi yao
ila fimbo tu,[m] **9** lakini wafunge viatu, na wasivae mavazi mawili ya ndani.[n] **10** Zaidi ya hayo, akawaambia: "Popote mtakapoingia katika nyumba,[o] kaeni humo mpaka
mtakapoondoka.[p] **11** Na ma-

SURA 5
a Lu 8:49
b 2Nya 20:20; Lu 8:50; Yoh 11:40
c Mt 17:1; Mt 26:37
d Mt 9:23; Lu 8:52; Yoh 11:11
e Mt 9:24; Lu 8:51; Lu 8:53
f Mt 9:25; Lu 7:14; Lu 8:54; Mdo 9:40
g Lu 8:55
h Mk 1:44; Mk 7:36

SURA 6
i Mt 13:54; Lu 4:16

Safu ya 2
a Mt 13:54; Yoh 6:42; Yoh 7:15
b Isa 53:2; 1Ko 1:23
c Yoh 6:42
d Ga 1:19
e Mk 3:31
f Mt 13:56
g Yer 11:21
h Mt 13:57; Lu 4:24; Yoh 4:44
i Mt 9:35; Mt 10:23; Lu 13:22
j Mhu 4:9; Lu 10:1
k Mt 10:1; Lu 9:1
l Ro 15:27; Ga 6:6
m Mt 10:9; Lu 9:3
n Mt 10:10; Mdo 12:8
o Mt 10:11
p Lu 9:4

hali popote ambapo hamtapo-
kewa wala kusikilizwa, mna-
poondoka yakung'uteni ma-
vumbi yaliyo chini ya miguu
yenu ili kuwa ushahidi kwao."[a]
12 Kwa hiyo wakaondoka na
kuhubiri ili watu wapate kutu-
bu;[b] **13** nao walikuwa waki-
toa roho waovu[c] wengi na ku-
wapaka mafuta[d] watu wengi
waliokuwa wagonjwa na ku-
waponya.[e]

14 Basi Mfalme Herode aka-
sikia, kwa maana jina la Yesu
lilikuwa limejulikana na watu
wote, na watu walikuwa waki-
sema: "Yohana mbatizaji ame-
fufuliwa kutoka kwa wafu,
na kwa sababu hiyo anatenda
kazi zenye nguvu."[f] **15** Laki-
ni wengine walikuwa wakise-
ma: "Ni Eliya."[g] Bado wengi-
ne walikuwa wakisema: "Ni
nabii kama mmoja wa mana-
bii."[h] **16** Lakini Herode ali-
posikia hilo akaanza kusema:
"Yohana ambaye nilimkata ki-
chwa, ndiye huyo amefufu-
liwa."[i] **17** Kwa maana Hero-
de mwenyewe alikuwa ame-
tuma watu wakamkamata Yo-
hana na kumfunga gerezani
kwa sababu ya Herodia mke
wa Filipo ndugu yake, kwa
sababu Herode alikuwa ame-
mwoa.[j] **18** Kwa maana Yoha-
na alikuwa amemwambia He-
rode tena na tena: "Si halali
wewe kuwa na mke wa ndugu
yako."[k] **19** Lakini Herodia
alikuwa na kinyongo[l] moyoni
kumwelekea na alikuwa aki-
taka kumuua, lakini hakuwe-
za.[m] **20** Kwa maana Herode
alikuwa akimwogopa[n] Yohana,
na alimjua kuwa mtu mwadili-
fu na mtakatifu;[o] naye alikuwa

SURA 6

a Mt 10:14
Lu 10:10
Mdo 13:51

b Mdo 2:38
Mdo 3:19

c Lu 10:17

d Yak 5:14

e Lu 9:6

f Mt 14:1
Lu 9:7

g Mk 8:28

h Mt 16:14
Lu 9:8

i Lu 9:9

j Mt 14:3
Lu 3:19

k Law 18:16
Law 20:21
Mt 14:4
Ebr 13:4

l Law 19:18

m Zb 37:32
Mt 14:5

n Mt 21:26

o Mt 11:11

Safu ya 2

a Mdo 24:24

b Mt 14:6

c Mwa 40:20

d Mk 2:15

e Est 5:6
Est 7:2

f Law 5:4
Mt 14:7

g Met 12:10
Mt 14:10

h Mt 14:9

i Mt 14:10

j Mt 14:11

akimlinda. Na baada ya kumsi-
kia[a] akawa hajui kabisa la ku-
fanya, lakini aliendelea kumsi-
kia kwa furaha.

21 Lakini siku inayofaa[b] ika-
fika wakati Herode alipoandaa
mlo wa jioni kwenye sikukuu
ya kuzaliwa[c] kwake kwa ajili
ya wenye daraja la juu na vi-
ongozi wake wa kijeshi na wa-
lio wa cheo cha kwanza ka-
bisa wa Galilaya. **22** Na bi-
nti ya Herodia huyohuyo aka-
ingia, akacheza dansi na
kumpendeza Herode na wale
wenye kuketi[d] pamoja naye.
Mfalme akamwambia mwana-
mwali huyo: "Niombe chochote
unachotaka, nami nitakupa."
23 Ndiyo, akamwapia: "Cho-
chote utakachoniomba, nita-
kupa hicho,[e] hata nusu ya ufa-
lme wangu."[f] **24** Naye akae-
nda akamwambia mama yake:
"Niombe nini?" Akamwambia:
"Kichwa cha Yohana mbatiza-
ji."[g] **25** Mara akaingia hara-
ka mpaka mahali alipokuwa
mfalme na kutoa ombi lake,
akisema: "Nataka unipe sasa
hivi kwenye sahani kichwa cha
Yohana Mbatizaji." **26** Ijapo-
kuwa mfalme alikuwa na hu-
zuni sana, lakini hakutaka ku-
mpuuza, kwa kufikiria vile vi-
apo na wale waliokuwa wame-
keti mezani.[h] **27** Kwa hiyo
mara moja mfalme akamtu-
ma mlinzi wa mfalme na ku-
mwamuru akalete kichwa cha-
ke. Naye akaenda akamkata
kichwa gerezani[i] **28** akakile-
ta kichwa chake kwenye sa-
hani, naye akampa yule mwa-
namwali, naye mwanamwali
akampa mama yake.[j] **29** Wa-
nafunzi wake waliposikia juu

ya hilo wakaja wakachukua
maiti yake na kuilaza katika
kaburi.[a]
30 Nao mitume wakakusa-
nyika pamoja mbele ya Yesu na
kumwambia mambo yote wa-
liyokuwa wamefanya na ku-
fundisha.[b] **31** Naye akawaam-
bia: "Njooni, ninyi wenyewe,
faraghani katika mahali pasi-
po na watu[c] mpumzike kido-
go."[d] Kwa maana watu wali-
kuwa wakija na kwenda, nao
hawakuwa hata na wakati wa
kula mlo.[e] **32** Kwa hiyo wa-
kaenda zao wakiwa katika ma-
shua wakawe peke yao kati-
ka mahali pasipo na watu.[f]
33 Lakini watu wakawaona
wakienda na wengi wakapata
kujua hilo, na kutoka katika
majiji yote wakakimbia pamo-
ja kwenda huko kwa miguu na
kufika mbele yao.[g] **34** Basi,
aliposhuka, akaona umati
mkubwa, lakini akawasikiti-
kia,[h] kwa sababu walikuwa
kama kondoo wasio na mchu-
ngaji.[i] Naye akaanza kuwafu-
ndisha mambo mengi.[j]
35 Kufikia wakati huo saa
ilikuwa imesonga sana, na wa-
nafunzi wake wakamjia na ku-
anza kusema: "Mahali hapa
hapana watu, na saa tayari
imesonga sana.[k] **36** Waache
waende zao, ili waende ma-
shambani na kwenye vijiji vi-
navyozunguka wakajinunulie
chakula."[l] **37** Akajibu aka-
waambia: "Ninyi wapeni cha-
kula." Ndipo wakamwambia:
"Je, twende tukanunue mika-
te yenye thamani ya dinari
mia mbili na kuwapa watu ili
wale?"[m] **38** Akawaambia:
"Mna mikate mingapi? Nende-
ni mkaone!" Baada ya kuha-
kikisha, wakasema: "Mitano,
na samaki wawili."[a] **39** Naye
akawaagiza watu wote wake-
ti wakiwa vikundi-vikundi[b] juu
ya majani mabichi.[c] **40** Nao
wakajilaza chini katika viku-
ndi vya watu 100 na vya watu
50.[d] **41** Sasa akaichukua ile
mikate mitano na wale sama-
ki wawili, akatazama juu mbi-
nguni akatoa baraka,[e] akaime-
ga[f] ile mikate na kuanza kuwa-
pa wanafunzi, ili wapate kui-
weka mbele ya watu hao; naye
akawagawanya wale samaki
wawili kwa ajili ya watu wote.
42 Kwa hiyo wote wakala, wa-
kashiba;[g] **43** nao wakaokota
vipande, vikapu kumi na viwi-
li vilivyojaa, mbali na wale sa-
maki. **44** Zaidi ya hayo, wale
waliokula ile mikate walikuwa
wanaume elfu tano.[h]
45 Na, bila kukawia, aka-
waagiza wanafunzi wake wa-
ipande mashua na kumtangu-
lia kwenda ukingo wa pili wa
bahari kuelekea Bethsaida,
huku yeye mwenyewe akiuru-
husu umati uende.[i] **46** Laki-
ni baada ya kuwaaga akaenda
mlimani ili asali.[j] **47** Sasa ili-
pokuwa jioni, mashua ilikuwa
katikati ya bahari, lakini
yeye alikuwa peke yake kwe-
nye nchi kavu.[k] **48** Na ali-
powaona wakitaabika[l] katika
kuvuta kwao makasia, kwa
maana upepo ulikuwa ukivu-
ma kinyume chao, karibu ke-
sha la nne la usiku akawaen-
dea, akitembea juu ya bahari;
lakini alitaka kuwapita.
49 Walipomwona akitembea
juu ya bahari wakafikiri: "Ni
mzuka!" nao wakapaaza sa-

SURA 6
a Mt 14:12
Mdo 8:2
b Lu 9:10
c Mt 14:13
d Mt 11:29
e Mk 3:20
f Yoh 6:1
g Lu 9:11
Yoh 6:2
h Mik 6:8
Mt 9:36
Mt 14:14
Ebr 4:15
i 1Fa 22:17
Isa 53:6
Eze 34:5
Mt 9:36
j Isa 61:1
Lu 9:11
k Mt 14:15
Lu 9:12
l Yoh 6:5
m Hes 11:13
2Fa 4:43
Mt 15:33
Yoh 6:7

Safu ya 2
a Mt 14:17
Lu 9:13
Yoh 6:9
b Mt 15:35
1Ko 14:40
c Mt 14:19
Yoh 6:10
d Lu 9:14
e 1Sa 9:13
Lu 24:30
1Ti 4:4
f Mt 26:26
Mk 8:6
Mdo 27:35
g Mt 14:20
Lu 9:17
Yoh 6:12
h Mt 14:21
Yoh 6:13
i Mt 14:22
Yoh 6:14
j Mt 6:6
Mt 14:23
Mk 1:35
Lu 6:12
k Mt 14:24
Yoh 6:16
l Yoh 6:19

uti kubwa.[a] **50** Kwa maana
wote walimwona, wakataabika.
Lakini mara moja akasema
nao, naye akawaambia: "Jipe-
ni moyo, ni mimi; msiogope."[b]
51 Naye akapanda na kuingia
katika mashua pamoja nao, na
upepo ukapungua. Ndipo wa-
kashangaa sana ndani yao we-
nyewe,[c] **52** kwa maana ha-
wakuwa wamefahamu maana
ya ile mikate, bali mioyo yao ili-
kuwa mizito isiweze kuelewa.[d]
53 Na walipovuka mpaka
nchi kavu, wakaingia Genesa-
reti na kutia meli nanga hapo
karibu.[e] **54** Lakini mara tu
waliposhuka kutoka katika
mashua, watu wakamtambua,
55 nao wakakimbia kuzungu-
ka eneo lote hilo na kuanza ku-
wachukua huku na huku juu
ya vitanda wale waliokuwa wa-
kiugua mpaka kule walikosi-
kia alikuwako. **56** Na kokote
alikokuwa akiingia vijijini au
majijini au mashambani[f] wa-
likuwa wakiweka wale wago-
njwa sokoni, nao walikuwa wa-
kiomba ili wapate kuugusa[g] tu
upindo[h] wa vazi lake la nje. Na
wote waliougusa wakapona.[i]

7 Sasa Mafarisayo na baa-
dhi ya waandishi waliokuwa
wamekuja kutoka Yerusa-
lemu wakakusanyika kumzu-
nguka.[j] **2** Nao walipoona ba-
adhi ya wanafunzi wake wakila
mlo wao kwa mikono najisi, ya-
ani, ambayo haijanawishwa[k]—
3 kwa maana Mafarisayo na
Wayahudi wote hawali isipo-
kuwa wawe wamenawa miko-
no yao mpaka kwenye kiwi-
ko, kwa kushika sana mapo-
keo ya watu wa nyakati za
hapo zamani, **4** na, wanapo-
rudi kutoka sokoni, hawali
chakula isipokuwa wawe wa-
mejisafisha kwa kunyunyiza;
na kuna mapokeo[a] mengine
mengi ambayo wamepokea ili
kushika sana, ubatizo wa viko-
mbe na mitungi na vyombo vya
shaba;[b]— **5** Kwa hiyo Mafa-
risayo na waandishi hao waka-
muuliza: "Kwa nini wanafunzi
wako hawajiendeshi kulingana
na mapokeo ya watu wa zama-
ni, bali hula mlo wao kwa miko-
no iliyo najisi?"[c] **6** Akawaa-
mbia: "Isaya kwa kufaa ali-
toa unabii juu yenu wanafiki,
kama ilivyoandikwa,[d] 'Watu
hawa huniheshimu mimi kwa
midomo yao, bali mioyo yao iko
mbali nami.[e] **7** Wao huniabu-
du bure, kwa sababu wao hu-
fundisha amri za wanadamu
kuwa mafundisho.'[f] **8** Mnai-
acha amri ya Mungu, na kuya-
shika sana mapokeo ya wana-
damu."[g]

9 Zaidi ya hayo, akaende-
lea kuwaambia: "Kwa ustadi
mnaweka kando amri[h] ya
Mungu kusudi mbaki na
mapokeo yenu. **10** Kwa mfa-
no, Musa alisema, 'Mheshi-
mu baba yako na mama
yako,'[i] na, 'Yule anayemtuka-
na baba yake au mama yake
na afe.'[j] **11** Lakini ninyi hu-
sema, 'Mtu akimwambia baba
yake au mama yake: "Chocho-
te nilicho nacho unachoweza
kufaidika nacho kutoka kwa-
ngu ni korbani,[k] (yaani, zawa-
di iliyowekwa wakfu[l] kwa Mu-
ngu,)"'— **12** Ninyi hammru-
husu afanye hata jambo moja
kwa ajili ya baba yake au mama
yake,[m] **13** na hivyo mnali-
batilisha neno la Mungu[n] kwa

SURA 6
a Lu 24:37 Yoh 6:19
b Mt 14:27 Yoh 6:20
c Mt 14:32 Yoh 6:21
d Mt 16:9 Mk 3:5 Mk 8:17
e Mt 14:34
f Mt 14:35
g Mt 9:20 Mk 5:27 Lu 8:44 Mdo 19:12
h Hes 15:38
i Mt 14:36

SURA 7
j Mt 15:1
k Lu 11:38

Safu ya 2
a Mt 15:6
b Mt 23:25 Lu 11:39
c Mt 15:2
d Mt 15:7
e Eze 33:31 Mt 15:8
f Isa 29:13 Mt 15:9 Kol 2:8
g Mt 15:3 Ga 1:14 Tit 1:14
h Isa 24:5
i Kut 20:12 Kum 5:16 Mt 15:4 Efe 6:2
j Kut 21:17 Law 20:9 Met 20:20
k Mt 15:5 Mt 23:18
l Law 1:2 Law 2:1
m 1Ti 5:8
n Mt 15:6

mapokeo yenu ambayo mlipewa. Nanyi hufanya mambo mengi[a] yanayofanana na hilo.”
14 Kwa hiyo, akiuita tena
umati kwake, akaendelea kuu-
ambia: “Nisikilizeni, ninyi nyo-
te, mpate maana.[b] **15** Haku-
na kitu chochote kutoka nje
ya mtu kinachoingia ndani
yake ambacho kinaweza ku-
mtia unajisi; bali mambo yana-
yotoka ndani ya mtu ndiyo ma-
mbo yanayomtia mtu unajisi.”[c]
16 ——

17 Basi alipokuwa ameingia
katika nyumba akiwa mbali
na umati, wanafunzi wake wa-
kaanza kumuuliza habari ya
mfano huo.[d] **18** Kwa hiyo
akawaambia: “Ninyi pia ha-
mna ufahamu kama wao?[e] Je,
hamjui kwamba hakuna cho-
chote kutoka nje kinachoingia
ndani ya mtu ambacho kina-
weza kumtia unajisi, **19** kwa
kuwa hicho hupita na kuingia,
si ndani ya moyo wake, bali
ndani ya matumbo yake, na-
cho hutoka nje na kuingia nda-
ni ya shimo la choo?”[f] Kwa
njia hiyo akatangaza vyaku-
la vyote kuwa safi.[g] **20** Tena
akasema: “Kile ambacho huto-
ka ndani ya mtu ndicho hu-
mtia mtu unajisi;[h] **21** kwa
maana kutoka ndani, kutoka
katika moyo wa watu,[i] huto-
ka mawazo mabaya: uasherati,[j]
wizi, mauaji,[k] **22** uzinzi, ku-
tamani,[l] matendo ya uovu, uda-
nganyifu, mwenendo mpoto-
vu,[m] jicho lenye wivu, makufu-
ru, majivuno, ukosefu wa akili.
23 Mambo hayo yote maovu
hutoka ndani nayo humtia mtu
unajisi.”[n]

24 Akatoka huko, akaenda

SURA 7
a Mk 7:3
b Met 8:5
Mt 15:10
c Mt 15:11
Mdo 10:14
1Ko 8:8
1Ti 4:4
Tit 1:15
d Mt 15:15
Lu 8:9
e Mt 15:16
f Mt 15:17
g Lu 11:41
Mdo 10:15
h Mt 15:18
i Mwa 6:5
Mwa 8:21
Zb 14:1
Yer 17:9
j Ga 5:19
k Mt 15:19
l Tit 3:3
m Ga 5:19
Efe 4:19
n Mt 15:20
Ro 1:28

Safu ya 2
a Mt 11:21
Mt 15:21
b Mk 2:1
c Mt 15:22
d Mt 15:22
e Mt 15:24
f Mt 7:6
Mt 10:5
Mt 15:26
Ro 9:4
Efe 2:12
g Lu 16:21
h Mt 15:27
i Mt 15:28
j Yoh 4:51
k Mt 15:29
Mk 5:20
l Mt 9:32
Lu 11:14
Mdo 9:12

katika maeneo ya Tiro na Sido-
ni.[a] Naye akaingia katika nyu-
mba wala hakutaka mtu yeyo-
te ajue. Na bado hakuweza ku-
epuka kutambuliwa;[b] **25** la-
kini mara moja mwanamke
ambaye binti yake mdogo ali-
kuwa na roho mchafu akasi-
kia habari zake akaja na kuji-
angusha chini miguuni pake.[c]
26 Yule mwanamke alikuwa
wa kutoka Ugiriki, wa tai-
fa la Sirofoinike; naye aka-
wa akimwomba amfukuze
roho mwovu kutoka katika
binti yake.[d] **27** Lakini akaa-
nza kumwambia mwanamke
huyo: “Kwanza acha watoto
washibe, kwa maana si sawa
kuuchukua mkate wa wato-
to[e] na kuwatupia mbwa wado-
go.”[f] **28** Hata hivyo, mwana-
mke huyo akajibu, akamwa-
mbia: “Ndiyo, bwana, lakini
hao mbwa wadogo walio chi-
ni ya meza hula sehemu ya
makombo[g] ya watoto wado-
go.”[h] **29** Ndipo akamwambia
mwanamke huyo: “Kwa saba-
bu umesema hivyo, nenda; yule
roho mwovu amemtoka binti
yako.”[i] **30** Kwa hiyo akaen-
da nyumbani kwake na ku-
mkuta[j] huyo mtoto mchanga
akiwa amelazwa kitandani na
roho mwovu amemtoka.

31 Basi alipokuwa akirudi
kutoka katika maeneo ya Tiro
akapitia Sidoni mpaka bahari
ya Galilaya akipanda na ku-
pita katikati ya maeneo ya De-
kapoli.[k] **32** Huko wakamle-
tea mtu aliye kiziwi na mwe-
nye kizuizi cha usemi, nao
wakamsihi aweke mkono wake
juu yake.[l] **33** Naye akamchu-
kua kutoka katika umati na

kumpeleka mahali pasipo na
watu akaweka vidole vyake
ndani ya masikio ya yule mtu
na, baada ya kutema mate, aka-
mgusa ulimi wake.[a] **34** Naye
akatazama juu mbinguni,[b] aka-
vuta pumzi[c] kwa nguvu na
kumwambia: *"Efatha,"* yaa-
ni, "Funguka." **35** Basi, uwe-
zo wake wa kusikia ukafungu-
ka,[d] na kile kifungo cha ulimi
wake kikafunguliwa, naye aka-
anza kusema kama kawaida.
36 Ndipo akawaamuru wasi-
mwambie yeyote;[e] lakini kwa
kadiri alivyozidi kuwawaamu-
ru, ndivyo walivyozidi kuta-
ngaza jambo hilo.[f] **37** Kwa
kweli, walikuwa wakistaaja-
bu[g] sana nao wakasema: "Ame-
fanya mambo yote vema.
Anafanya hata viziwi wasi-
kie na wasioweza kusema,
waseme."[h]

8 Siku hizo, kulipokuwa
tena na umati mkubwa nao
haukuwa na chakula, akawa-
ita wanafunzi na kuwaambia:[i]
2 "Ninausikitikia[j] umati, kwa
sababu tayari wamekaa nami
siku tatu nao hawana chaku-
la; **3** nami nikiwaambia wa-
ende nyumbani kwao wakiwa
wamefunga, watazimia bara-
barani. Kwa kweli, baadhi yao
wanatoka mbali." **4** Lakini
wanafunzi wake wakamjibu:
"Mtu yeyote aliye mahali hapa
pasipo na watu atawashibisha
watu hawa kwa mikate kutoka
wapi?"[k] **5** Na bado akaende-
lea kuwauliza: "Mna mikate
mingapi?" Wakasema: "Saba."[l]
6 Naye akauagiza umati uketi
chini, naye akaichukua ile mi-
kate saba, akashukuru,[m] akai-
mega, na kuanza kuwapa wa-

SURA 7
a Mk 8:23
Yoh 9:6
b Mk 6:41
Yoh 17:1
c Yoh 11:33
Yoh 11:38
d Isa 35:5
Mt 11:5
Mt 15:30
e Isa 42:2
Mt 8:4
Mk 5:43
f Mk 1:45
g Mdo 14:11
h Isa 35:5
Mt 15:31

SURA 8
i Mt 15:32
j Ebr 2:17
Ebr 4:15
Ebr 5:2
k Hes 11:21
2Fa 7:2
Mt 15:33
Mk 6:52
l Mt 15:34
Mk 6:38
m Kum 8:10
Lu 22:19
1Ti 4:4

Safu ya 2
a Mt 15:36
Mk 6:41
b Mt 14:19
c Mt 15:37
d Mt 15:38
e Mt 15:39
f Mt 12:38
Mt 16:1
Yoh 6:30
g Mk 7:34
h Mt 16:4
i Mt 16:5
j Mt 16:6
Lu 12:1
1Ko 5:7
Ga 5:9
k Mt 16:7
l Yoh 4:33
m Isa 29:24
Mt 16:8
Mk 6:52

nafunzi wake waigawe, nao
wakaugawia umati.[a] **7** Wali-
kuwa pia na samaki wadogo
wachache; na, akiisha kuwa-
bariki, akawaambia wawaga-
we hao pia.[b] **8** Basi wakala
na kushiba, nao wakaokota zi-
ada ya vipande vidogo, vikapu
saba vya chakula vilivyojaa.[c]
9 Ingawa kulikuwa na karibu
wanaume elfu nne. Mwishowe
akawaacha waende zao.[d]

10 Na mara akaipanda ma-
shua pamoja na wanafunzi
wake akaingia katika zile sehe-
mu za Dalmanutha.[e] **11** Taza-
ma, Mafarisayo wakatokea na
kuanza kubishana naye, wa-
kitafuta kwake ishara kuto-
ka mbinguni, ili kumjaribu.[f]
12 Kwa hiyo akaugua sana[g] ro-
honi mwake, na kusema: "Kwa
nini kizazi hiki kinatafuta isha-
ra? Kwa kweli mimi ninasema,
Kizazi hiki hakitapewa isha-
ra yoyote."[h] **13** Ndipo akawa-
acha, akapanda ndani tena, na
kwenda mpaka ukingo wa pili
wa bahari.

14 Ikawa kwamba walisa-
hau kuichukua mikate, na ha-
wakuwa na kitu katika mashua
ila mkate mmoja.[i] **15** Naye
akaanza kuwaagiza waziwa-
zi na kusema: "Endeleeni ku-
fungua macho yenu, jihadhari-
ni na chachu ya Mafarisayo na
chachu ya Herode."[j] **16** Kwa
hiyo wakaanza kubishana kwa
sababu hawakuwa na mikate
yoyote.[k] **17** Akijua hilo, aka-
waambia: "Kwa nini mnabi-
shana kwa sababu hamna mi-
kate?[l] Je, bado hamjaelewa
wala kupata maana? Je, mio-
yo yenu ni mizito isiweze kue-
lewa?[m] **18** 'Ijapokuwa mna

macho, hamwoni; na ijapokuwa mna masikio, hamsikii?'[a]
Na je, hamkumbuki, **19** wakati nilipoimega ile mikate mitano[b] kwa ajili ya wale wanaume elfu tano, mliokota vikapu vingapi vilivyokuwa vimejaa vipande?" Wakamwambia:
"Kumi na viwili."[c] **20** "Nilipoimega ile mikate saba kwa ajili
ya wale wanaume elfu nne, mliokota vikapu vingapi vya chakula vilivyokuwa vimejaa vipande?" Nao wakamwambia:
"Saba."[d] **21** Ndipo akawaambia: "Je, bado hamjapata maana?"[e]

22 Sasa wakafika Bethsaida. Tazama, watu wakamletea mtu aliye kipofu, nao wakamsihi amguse.[f] **23** Naye akamshika mkono yule mtu aliyekuwa kipofu, akamtoa nje ya kijiji, na, baada ya kutema mate[g] juu ya macho yake, Yesu akaweka mikono juu yake na kuanza kumuuliza: "Je, unaona kitu chochote?" **24** Na yule mtu akatazama juu na kuanza kusema: "Ninaona watu, kwa sababu ninaona vitu vinavyoonekana kama miti, lakini vinatembea huku na huku." **25** Kisha akaweka mikono yake tena juu ya macho ya mtu huyo, na mtu huyo akaona waziwazi, naye akapona, naye alikuwa akiona kila kitu waziwazi. **26** Kwa hiyo akamwagiza aende nyumbani, akisema: "Lakini usiingie kijijini."[h]

27 Yesu na wanafunzi wake wakaondoka kwenda vijiji vya Kaisaria Filipi, na njiani akaanza kuwauliza wanafunzi wake, akisema: "Watu wanasema mimi ni nani?"[a] **28** Wakamwambia: "Yohana Mbatizaji,[b] na wengine, Eliya,[c] na wengine bado, Mmoja wa manabii."[d]
29 Naye akawauliza: "Ingawa hivyo, ninyi mnasema mimi ni nani?" Petro akajibu akamwambia: "Wewe ndiye Kristo."[e]
30 Ndipo akawapa onyo kali wasimwambie mtu yeyote juu yake.[f] **31** Pia, akaanza kuwafundisha kwamba Mwana wa binadamu lazima apatwe na mateso mengi na kukataliwa na wanaume wazee na wakuu wa makuhani na waandishi na kuuawa,[g] na kufufuka siku tatu baadaye.[h] **32** Kwa kweli, alikuwa akisema hayo waziwazi. Lakini Petro akamchukua kando na kuanza kumkemea.[i] **33** Akageuka, akawatazama wanafunzi wake, akamkemea Petro, na kusema: "Nenda nyuma yangu, Shetani, kwa sababu wewe unafikiri, si fikira za Mungu, bali za wanadamu."[j]

34 Basi akauita umati pamoja na wanafunzi wake na kuwaambia: "Mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe na kuuchukua mti wake wa mateso na kunifuata sikuzote.[k] **35** Kwa maana yeyote yule anayetaka kuiokoa nafsi yake ataipoteza; lakini yeyote yule anayeipoteza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya habari njema ataiokoa.[l] **36** Kwa kweli, mtu anapata faida gani ikiwa ataupata ulimwengu wote na kuipoteza nafsi yake?[m] **37** Kwa kweli, mtu anaweza kutoa nini ili aipate nafsi yake?[n] **38** Kwa maana mtu yeyote yule ana-

SURA 8
a Isa 44:18; Yer 5:21; Eze 12:2; Mt 13:13
b Mk 6:38
c Mt 14:20; Mk 6:43; Lu 9:17; Yoh 6:13
d Mt 15:37
e Mt 16:11; Mk 6:52
f Mk 6:56
g Mk 7:33; Yoh 9:6
h Mt 8:4; Mk 5:43

Safu ya 2
a Mt 16:13; Lu 9:18
b Mt 14:2; Mk 6:14
c Mk 9:11
d Mt 16:14; Lu 9:19
e Mt 16:16; Lu 9:20; Yoh 1:41; Yoh 6:69; 1Yo 4:15
f Mt 16:20; Mk 9:9; Lu 9:21
g Mt 26:2
h Mt 16:21; Mt 17:23; Lu 9:22
i Mt 16:22
j Mt 16:23; Ro 8:7; 1Ko 2:14
k Mt 10:38; Mt 16:24; Lu 9:23; Lu 14:27; Ga 5:24
l Mt 10:39; Mt 16:25; Lu 9:24; Yoh 12:25; Ufu 12:11
m Mt 16:26; Lu 9:25
n Zb 49:8

yenionea aibu mimi na maneno
yangu katika kizazi hiki che-
nye uzinzi na chenye dhambi,
Mwana wa binadamu atamwo-
nea aibu[a] yeye pia atakapofika
katika utukufu wa Baba yake
pamoja na malaika watakatifu."[b]

9 Zaidi ya hayo, akaende-
lea kuwaambia: "Kwa kwe-
li ninawaambia ninyi, Kuna
baadhi ya wale wanaosimama
hapa ambao hawataonja kifo
kamwe mpaka kwanza wauo-
ne ufalme wa Mungu ukiwa ta-
yari umekuja katika nguvu."[c]
2 Basi siku sita baadaye Yesu
akawachukua Petro na Yakobo
na Yohana pamoja naye, aka-
wapandisha katika mlima mre-
fu wakiwa peke yao. Sura yake
ikageuka mbele yao,[d] **3** na
mavazi yake ya nje yakame-
tameta, yakawa meupe kuliko
vile msafisha-nguo yeyote du-
niani anavyoweza kuyafanya.[e]
4 Pia, Eliya na Musa wakawa-
tokea, nao walikuwa wakio-
ngea na Yesu.[f] **5** Petro akaji-
bu, akamwambia Yesu: "Rabi,
ni vizuri kwetu kuwa hapa,
kwa hiyo na tusimamishe ma-
hema matatu, moja lako na
moja la Musa na moja la Eli-
ya."[g] **6** Kwa kweli, hakujua
ajibu nini, kwa maana waliogopa sana. **7** Na wingu lika-
tokea, likawafunika, na sauti[h] ikatoka katika lile wingu:
"Huyu ni Mwanangu,[i] mpendwa; msikilizeni."[j] **8** Hata
hivyo, kwa ghafula wakatazama huku na huku nao hawa-
kumwona yeyote pamoja nao
tena, ila Yesu peke yake.[k]

9 Walipokuwa wakishuka
kutoka kwenye ule mlima, aka-
waagiza waziwazi wasimsimu-
lie[a] mtu yeyote kile walicho-
ona, mpaka baada ya Mwana
wa binadamu kufufuka kuto-
ka kwa wafu.[b] **10** Nao wa-
kalitia neno hilo moyoni,
lakini wakazungumza katikati
yao wenyewe maana ya kufu-
fuliwa huko kutoka kwa wafu.
11 Nao wakaanza kumuuliza,
wakisema: "Kwa nini waandi-
shi husema kwamba lazima
Eliya[c] aje kwanza?"[d] **12** Aka-
waambia: "Eliya anakuja kwa-
nza na kurudisha mambo
yote;[e] lakini kwa nini imea-
ndikwa juu ya Mwana wa bi-
nadamu kwamba lazima apa-
twe na mateso mengi[f] na kute-
ndewa kama asiye wa maana?[g]
13 Lakini mimi ninawaambia
ninyi, Eliya,[h] kwa kweli, ame-
kuja, nao walimtendea mam-
bo mengi kama walivyota-
ka, kama ilivyoandikwa juu
yake."[i]

14 Sasa, walipowakaribia
wale wanafunzi wengine, wa-
kaona umati mkubwa umewa-
zunguka na waandishi waki-
bishana nao.[j] **15** Lakini mara
tu umati wote ulipomwona
ukashangaa, ukamkimbilia, na
kuanza kumsalimu. **16** Naye
akawauliza: "Mnabishania nini
nao?" **17** Na mmoja kutoka
katika ule umati akamjibu:
"Mwalimu, nilileta mwanangu
kwako kwa sababu ana roho
bubu;[k] **18** na popote pale ana-
pomkamata humwangusha chi-
ni, naye hutoa povu na kusaga
meno yake na kupoteza nguvu
zake. Nami niliwaambia wana-
funzi wako wamfukuze, laki-
ni hawakuweza."[l] **19** Akaji-
bu akawaambia: "Enyi kizazi

SURA 8

a Mt 10:33
Mt 16:27
Lu 9:26
Lu 12:9
Ro 1:16
2Ti 1:8
b Mt 25:31
2Th 1:7

SURA 9

c Mt 16:28
Lu 9:27
1Ko 4:20
d Mt 17:1
Lu 9:28
e Da 7:9
Mt 17:2
Mt 28:3
Lu 9:29
f Mt 17:3
Lu 9:30
g Mt 17:4
Lu 9:33
h Lu 3:22
Yoh 12:28
i Zb 2:7
Isa 42:1
Mt 3:17
j Kum 18:15
Mt 17:5
Lu 9:35
Mdo 3:22
2Pe 1:17
k Mt 17:8
Lu 9:36

Safu ya 2

a Mt 12:16
Mk 8:30
b Mt 17:9
Lu 9:36
c Mal 4:5
Mk 8:28
d Mt 17:10
e Mt 17:11
f Mwa 3:15
Zb 22:6
Isa 50:6
Isa 53:3
Da 9:26
g Lu 23:11
Flp 2:7
h Mt 11:14
Lu 1:17
i Mt 17:12
j Lu 9:37
k Mt 17:14
Lu 9:38
l Mt 17:15
Lu 9:39

kisicho na imani,[a] nitaendelea
kuwa pamoja nanyi mpaka wa-
kati gani? Nitawavumilia ni-
nyi mpaka wakati gani? Mlete-
ni hapa."[b] **20** Kwa hiyo waka-
mpeleka mahali alipokuwa. La-
kini alipomwona tu, mara moja
yule roho akamfanya yule mto-
to agaegae, na baada ya kua-
nguka chini akajiviringisha,
akitoa povu.[c] **21** Naye aka-
muuliza baba yake: "Amekuwa
hivi kwa muda gani?" Akase-
ma: "Tangu utoto na kuende-
lea; **22** na mara kwa mara ali-
kuwa akimtupa ndani ya moto
na ndani ya maji ili kumwanga-
miza.[d] Lakini ikiwa unaweza
kufanya jambo lolote, utusiki-
tikie na kutusaidia." **23** Yesu
akamwambia: "Maneno hayo,
'Ikiwa unaweza'! Mambo yote
yanawezekana kwa mtu iki-
wa ana imani."[e] **24** Mara
moja baba ya yule mtoto mcha-
nga akapaaza sauti, akasema:
"Nina imani! Unisaidie maha-
li ambapo ninahitaji imani!"[f]
25 Yesu, sasa akiona kwa-
mba umati ulikuwa ukikimbia
kuwaelekea, akamkemea[g] yule
roho mchafu, akamwambia:
"Wewe roho bubu na kizi-
wi, ninakuagiza, toka ndani
yake wala usimwingie tena."
26 Na baada ya kupaaza sau-
ti na kugaagaa sana roho huyo
akatoka;[h] naye mtoto akawa ni
kama amekufa, hivi kwamba
wengi kati yao wakawa wa-
kisema: "Amekufa!" **27** La-
kini Yesu akamshika mkono
na kumwinua, naye akainu-
ka.[i] **28** Kwa hiyo baada ya
kuingia katika nyumba, wa-
nafunzi wake wakaanza ku-
muuliza faraghani: "Kwa nini
sisi hatukuweza kumfukuza?"[a]
29 Naye akawaambia: "Haku-
na chochote kinachoweza ku-
mtoa roho wa aina hii isipoku-
wa sala."[b]
30 Kutoka huko wakapitia
Galilaya, lakini hakutaka mtu
yeyote ajue. **31** Kwa maa-
na alikuwa akifundisha wana-
funzi wake na kuwaambia:
"Mwana wa binadamu atatiwa
mikononi mwa watu, nao wata-
muua, lakini, ijapokuwa atau-
awa,[c] atafufuka siku tatu baa-
daye."[d] **32** Hata hivyo, wali-
kuwa hawaelewi maneno hayo,
nao waliogopa kumuuliza.[e]
33 Nao wakaingia Kaper-
naumu. Sasa alipokuwa nda-
ni ya nyumba akawauliza:
"Mlikuwa mkibishania nini ba-
rabarani?"[f] **34** Wakakaa ki-
mya, kwa maana barabara-
ni walikuwa wamebishana we-
nyewe, ni nani aliye mkuu zai-
di.[g] **35** Kwa hiyo akaketi na
kuwaita wale kumi na wawi-
li na kuwaambia: "Ikiwa mtu
yeyote anataka kuwa wa kwa-
nza, lazima awe wa mwisho
kati ya wote na mhudumu wa
wote."[h] **36** Naye akamchu-
kua mtoto mchanga, akamsi-
mamisha katikati yao, aka-
mkumbatia na kuwaambia:[i]
37 "Yeyote yule anayempokea
mmoja wa watoto wachanga
kama huyu kwa msingi wa jina
langu, ananipokea mimi; na ye-
yote anayenipokea mimi, ana-
pokea, si mimi tu, bali pia yule
aliyenituma."[j]
38 Yohana akamwambia:
"Mwalimu, tulimwona mtu fu-
lani akitoa roho waovu kwa ku-
tumia jina lako nasi tukajaribu
kumzuia,[k] kwa sababu hakuwa

SURA 9

a Kum 32:20
b Mt 17:17
Lu 9:41
c Mk 1:26
Lu 9:42
d Mt 17:15
e 2Nya 20:20
Mt 17:20
Mk 11:23
Lu 17:6
Yoh 11:40
Mdo 14:9
f Lu 17:5
Efe 2:8
Ebr 12:2
g Mt 17:18
Mk 1:25
Lu 4:35
Mdo 10:38
h Mk 1:26
i Lu 9:42

Safu ya 2

a Mt 17:19
b Mt 17:20
c Mt 17:22
Mt 26:2
d Mt 16:21
Mt 17:23
Mk 8:31
Lu 9:44
e Lu 9:45
Yoh 16:19
f Mt 18:1
Lu 9:46
Lu 22:24
g Met 13:10
h Mt 18:1
Mt 20:28
Mk 10:43
Lu 9:46
Flp 2:8
i Mt 18:2
Mk 10:16
Lu 9:47
Lu 18:16
j Mt 10:40
Mt 18:3
Lu 9:48
Yoh 13:20
k Hes 11:28
Mdo 19:13

akifuatana nasi."[a] **39** Lakini
Yesu akasema: "Msijaribu ku-
mzuia, kwa maana hakuna ye-
yote atakayefanya matendo ye-
nye nguvu kwa msingi wa jina
langu ambaye ataweza kunitu-
kana upesi-upesi;[b] **40** kwa
maana mtu ambaye hatupingi
yuko upande wetu.[c] **41** Kwa
maana yeyote anayewapa ni-
nyi kikombe[d] cha maji ya ku-
nywa kwa sababu ninyi ni watu
wa Kristo,[e] kwa kweli ninawaa-
mbia ninyi, hatapoteza kamwe
thawabu yake. **42** Lakini ye-
yote anayemkwaza mmoja wa
hawa wadogo wanaoamini,
ingekuwa afadhali ikiwa jiwe
la kusagia kama lile ambalo hu-
zungushwa na punda lingewe-
kwa shingoni pake naye atu-
pwe baharini.[f]

43 "Na mkono wako uki-
kufanya ukwazike, ukate; ni
afadhali uingie katika uzima
ukiwa kilema kuliko kwenda
ukiwa na mikono miwili na
kuingia katika Gehena,* kati-
ka moto usioweza kuzimwa.[g]
44 —— **45** Na ikiwa mguu
wako unakufanya ukwazi-
ke, ukate; ni afadhali uingie
katika uzima ukiwa kilema[h]
kuliko kutupwa katika Gehe-
na* ukiwa na miguu miwi-
li.[i] **46** —— **47** Na ikiwa ji-
cho lako linakufanya ukwazike,
litupe mbali;[j] ni afadhali uingie
katika ufalme wa Mungu uki-
wa na jicho moja kuliko kutu-
pwa katika Gehena*[k] ukiwa
na macho mawili, **48** mahali
ambapo funza wake hafi na ule
moto hauzimwi.[l]

Mk 9:43,* 45,* 47* Bonde la Hinomu. Tazama Nyongeza 2.

SURA 9
a Lu 9:49
b 1Ko 12:3
c Mt 12:30
Lu 9:50
Lu 11:23
d Mt 10:42
Mt 25:35
e Mt 25:40
Ro 8:9
2Ko 10:7
f Mt 18:6
Lu 17:1
g Mt 5:30
Kol 3:5
h Mt 18:8
i Mt 10:28
Mt 23:33
Lu 12:5
j Mt 5:29
Mt 18:9
Ro 8:13
Ga 5:24
k Ufu 21:8
l Isa 66:24

Safu ya 2
a Lu 17:29
b Mt 5:13
Lu 14:34
c Met 15:1
Met 16:23
Kol 4:6
d Ro 12:18
Efe 4:29
1Th 5:13
Ebr 12:14

SURA 10
e Mt 19:1
Yoh 10:40
f Mal 2:16
Mt 19:3
g Kum 24:1
Mt 5:31
Mt 19:7
h Kum 9:6
Mdo 13:18
i Mwa 1:27
Mwa 5:2
Mt 19:4
j Mwa 2:24
Efe 5:31
k Mt 19:6
l Mk 9:28
m Mt 5:32
Mt 19:9
Lu 16:18

49 "Kwa maana kila mtu la-
zima atiwe chumvi[a] kwa moto.
50 Chumvi ni nzuri; lakini
chumvi ikipoteza nguvu zake,
mtaikoleza na nini?[b] Iweni na
chumvi[c] ndani yenu, na mdu-
mishe amani[d] kati ya mtu na
mwenzake."

10 Kutoka hapo akaondoka
na kuja kwenye mipaka
ya Yudea na ng'ambo ya Yo-
rdani, na tena umati ukamjia,
na kama alivyokuwa na de-
sturi ya kufanya akaanza tena
kuwafundisha.[e] **2** Mafarisa-
yo sasa wakamkaribia na, ili
kumjaribu, wakaanza kumuuli-
za kama ni halali mwanamume
kumtaliki mke wake.[f] **3** Aka-
jibu akawaambia: "Musa aliwaa-
muru ninyi nini?" **4** Wakase-
ma: "Musa aliruhusu kuandika
cheti cha kufukuza na kumta-
liki."[g] **5** Lakini Yesu akawaa-
mbia: "Kwa kufikiria ugumu
wenu wa moyo[h] aliwaandikia
ninyi amri hiyo. **6** Hata hi-
yo, tangu mwanzo wa kuumba
'Yeye aliwafanya mwanamume
na mwanamke.[i] **7** Kwa hiyo
mwanamume atamwacha baba
yake na mama yake, **8** na hao
wawili watakuwa mwili mmo-
ja';[j] hivi kwamba wao si wa-
wili tena, bali mwili mmoja.
9 Kwa hiyo kile ambacho Mu-
ngu ameunganisha mtu yeyo-
te asikitenganishe."[k] **10** Ali-
pokuwa tena katika nyumba[l]
wanafunzi wakaanza kumuuli-
za kuhusu hilo. **11** Naye aka-
waambia: "Mtu yeyote anaye-
mtaliki mke wake na kumwoa
mwingine anafanya uzinzi[m] dhi-
di yake, **12** na mwanamke,
baada ya kumtaliki mume

wake, akiolewa na mwingine,
anafanya uzinzi."[a]
13 Sasa watu wakaanza ku-
mletea watoto wachanga ili
awaguse; lakini wanafunzi wa-
kawakemea.[b] **14** Alipoona
hilo, Yesu akaghadhibika na
kuwaambia: "Waacheni watoto
wachanga waje kwangu; msija-
ribu kuwazuia, kwa maana ufa-
lme wa Mungu ni wa wale wa-
lio kama hao.[c] **15** Kwa kweli
ninawaambia ninyi, Yeyote yule
asiyeupokea ufalme wa Mu-
ngu kama mtoto mchanga ha-
taingia kamwe ndani yake."[d]
16 Naye akachukua watoto
akawakumbatia na kuanza ku-
wabariki, akiweka mikono yake
juu yao.[e]
17 Naye alipokuwa akito-
ka aende, mtu fulani aka-
mkimbilia akapiga magoti
mbele yake na kumuuliza:
"Mwalimu Mwema, nifanye
nini ili niurithi uzima wa mi-
lele?"[f] **18** Yesu akamwambia:
"Kwa nini unaniita mwema?[g]
Hakuna mtu aliye mwema,
ila mmoja, Mungu.[h] **19** Wewe
unazijua amri, 'Usiue,[i] Usifanye
uzinzi,[j] Usiibe,[k] Usitoe usha-
hidi wa uwongo,[l] Usipunje,[m]
Mheshimu baba yako na mama
yako.'"[n] **20** Mtu huyo aka-
mwambia: "Mwalimu, mambo
yote hayo nimeyashika tangu
ujana wangu na kuendelea."
21 Yesu akamtazama akampe-
nda na kumwambia: "Umeko-
sa jambo moja: Nenda, ukauze
vitu ulivyo navyo uwape ma-
skini, nawe utakuwa na hazina
mbinguni, kisha uje uwe mfua-
si wangu."[o] **22** Lakini akasi-
kitishwa na neno hilo na kwe-
nda zake akiwa amehuzunika,

SURA 10

a Ro 7:3
1Ko 7:13
b Mt 19:13
Lu 18:15
c Mt 18:4
Mt 19:14
Lu 18:16
1Pe 2:2
d Mt 18:3
Lu 18:17
e Mwa 48:14
Mk 9:36
f Mt 19:16
Lu 18:18
g Zb 86:5
h Mt 19:17
Lu 18:19
i Kut 20:13
Kum 5:17
Mt 5:21
1Yo 3:15
j Kut 20:14
Kum 5:18
k Kut 20:15
Kum 5:19
l Kut 20:16
Kum 5:20
m Law 19:13
n Kut 20:12
Kum 5:16
Efe 6:2
o Mt 19:21

Safu ya 2

a Lu 18:23
b Ayu 31:24
Zb 17:14
Zb 52:7
Zb 62:10
Yer 9:23
1Ti 6:17
c Mt 19:24
Lu 18:25
d Lu 4:32
e Mt 19:24
Lu 18:25
f Mt 19:25
Lu 18:26
1Pe 4:18
g Mwa 18:14
Ayu 42:2
Yer 32:17
Zek 8:6
Lu 18:27
h Mt 19:27
Lu 18:28
i Mt 10:37
Mt 19:29
Lu 18:29
j Lu 18:30
k Mt 5:11
Yoh 16:22
Mdo 14:22
l Mt 19:30
Mt 20:16
Lu 13:30

kwa maana alikuwa na mali
nyingi.[a]
23 Baada ya kutazama huku
na huku Yesu akawaambia
wanafunzi wake: "Jinsi ita-
kavyokuwa vigumu kwa wale
wenye pesa[b] kuingia katika
ufalme wa Mungu!"[c] **24** La-
kini wanafunzi wakashangaa[d]
kwa sababu ya maneno yake.
Yesu akajibu akawaambia tena:
"Wanangu, jinsi ilivyo vigu-
mu kuingia katika ufalme
wa Mungu! **25** Ni rahisi zai-
di ngamia kupita katika tu-
ndu la sindano kuliko tajiri
kuingia katika ufalme wa Mu-
ngu."[e] **26** Bado wakazidi ku-
staajabu na kumwambia: "Ni
nani ambaye, kwa kweli, ana-
weza kuokolewa?"[f] **27** Aki-
watazama moja kwa moja Yesu
akasema: "Kwa wanadamu ha-
iwezekani, lakini sivyo ilivyo
kwa Mungu, kwa maana mam-
bo yote yanawezekana kwa
Mungu."[g] **28** Petro akaanza
kumwambia: "Tazama! Sisi tuli-
acha vitu vyote na tumekuwa
tukikufuata wewe."[h] **29** Yesu
akasema: "Kwa kweli ninawaa-
mbia ninyi, Hakuna mtu amba-
ye ameacha nyumba au ndugu
au dada au mama au baba au
watoto au mashamba kwa aji-
li yangu na kwa ajili ya habari
njema[i] **30** ambaye hatapata
mara mia[j] sasa katika kipindi
hiki cha wakati, nyumba na
ndugu na dada na mama na
watoto na mashamba, pamoja
na mateso,[k] na katika mfumo
wa mambo unaokuja uzima wa
milele. **31** Hata hivyo, wengi
walio wa kwanza watakuwa wa
mwisho, na wa mwisho wataku-
wa wa kwanza."[l]

32 Sasa walikuwa barabarani, wakipanda kwenda Yerusalemu, na Yesu alikuwa akienda mbele yao, nao wakashangaa; lakini wale waliofuata wakaanza kuogopa. Mara nyingine tena akawachukua wale kumi na wawili kando na kuanza kuwaambia mambo haya yatakayompata:[a] **33** "Tazama, tunapanda kwenda Yerusalemu, na Mwana wa binadamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani, na waandishi, nao watamhukumia kifo na kumtia mikononi mwa watu wa mataifa,[b] **34** nao watamdhihaki, watamtemea mate, watampiga mijeledi na kumuua, lakini siku tatu baadaye atafufuka."[c]

35 Na Yakobo na Yohana, wana wawili wa Zebedayo,[d] wakamwendea na kumwambia: "Mwalimu, tunataka utufanyie chochote tutakachokuomba."[e] **36** Akawaambia: "Mnataka niwafanyie nini?" **37** Wakamwambia: "Uturuhusu kuketi, mmoja kwenye mkono wako wa kuume na mmoja kwenye mkono wako wa kushoto, katika utukufu wako."[f] **38** Lakini Yesu akawaambia: "Hamjui kile mnachoomba. Je, mnaweza kunywa kikombe ambacho ninakunywa, au kubatizwa kwa ubatizo ninaobatizwa?"[g] **39** Wakamwambia: "Tunaweza." Ndipo Yesu akawaambia: "Kikombe ninachokunywa mtakunywa, na ubatizo ninaobatizwa mtabatizwa.[h] **40** Hata hivyo, kuketi kwenye mkono wangu wa kuume au kwenye mkono wangu wa kushoto sina haki kutoa,[i] bali

SURA 10

a Mk 8:31
Mk 9:31
Lu 9:22
Lu 18:31
b Mt 20:18
Lu 18:31
c Mt 20:19
Lu 18:33
Mdo 10:40
1Ko 15:4
d Mt 10:2
e Mt 20:20
f Mt 19:28
Mt 20:21
g Mt 20:22
Lu 12:50
Yoh 18:11
Ro 6:3
h Mt 20:23
Mdo 12:2
Ufu 1:9
i Yak 4:3

Safu ya 2

a Mt 20:24
b Mt 20:25
Lu 22:25
1Pe 5:3
c Mt 20:26
Mk 9:35
Lu 9:48
d Mt 20:27
Lu 22:26
e Yoh 13:14
Flp 2:7
f Isa 53:10
Da 9:24
2Ko 5:21
Ga 3:13
Tit 2:14
g Law 16:17
Mt 20:28
h Mt 20:29
Lu 18:35
i Yer 23:5
Mt 9:27
Mt 15:22
Ro 1:3
j Lu 18:38
k Mt 20:31
Lu 18:39
l Mt 20:32
Lu 18:40

wataketi wale ambao wametayarishiwa."

41 Basi, wale wengine kumi waliposikia jambo hilo, wakaanza kuwaghadhibikia Yakobo na Yohana.[a] **42** Lakini Yesu, baada ya kuwaita, akawaambia: "Mnajua kwamba wale ambao huonekana kuwa wanatawala mataifa hupiga ubwana juu yao na wakuu wao hutumia mamlaka juu yao.[b] **43** Hivyo sivyo ilivyo katikati yenu; bali yeyote yule anayetaka kuwa mkubwa katikati yenu lazima awe mhudumu wenu,[c] **44** na yeyote yule anayetaka kuwa wa kwanza katikati yenu lazima awe mtumwa wa wote.[d] **45** Kwa maana hata Mwana wa binadamu alikuja, si kuhudumiwa,[e] bali kuhudumu na kutoa nafsi yake iwe fidia[f] badala ya wengi."[g]

46 Nao wakaingia Yeriko. Lakini yeye na wanafunzi wake na umati mkubwa walipokuwa wakitoka Yeriko, Bartimayo (mwana wa Timayo), kipofu aliye mwombaji, alikuwa ameketi kando ya barabara.[h] **47** Aliposikia kwamba ni Yesu Mnazareti, akaanza kupaaza sauti na kusema: "Mwana wa Daudi,[i] Yesu, unirehemu!"[j] **48** Ndipo wengi wakaanza kumwambia kwa ukali anyamaze; lakini akazidi kupaaza sana sauti: "Mwana wa Daudi, unirehemu!"[k] **49** Kwa hiyo Yesu akasimama na kusema: "Mwiteni." Nao wakamwita yule mtu aliye kipofu, wakamwambia: "Jipe moyo, simama, anakuita."[l] **50** Akatupa vazi lake la nje, akaruka na kusimama

kwa miguu yake, akamwendea
Yesu. **51** Yesu akamjibu, aka-
sema: “Unataka nikufanyie
nini?”[a] Yule mtu aliye kipofu
akamwambia: *“Raboni,* acha
nipate tena kuona.”[b] **52** Na
Yesu akamwambia: “Nenda,
imani yako imekuponya.”[c] Na
mara moja akapata tena ku-
ona,[d] naye akaanza kumfuata
barabarani.[e]

11 Walipokuwa wakikari-
bia kufika Yerusalemu,
Bethfage na Bethania[f] kwe-
nye Mlima wa Mizeituni, aka-
tuma wawili kati ya wanafu-
nzi wake[g] **2** na kuwaambia:
“Nendeni mkaingie katika kiji-
ji mnachokiona mbele yenu, na
mara tu mtakapoingia ndani
mtamkuta mwana-punda aki-
wa amefungwa, ambaye haku-
na mwanadamu yeyote amepa-
ta kuketi juu yake; mfungue-
ni mkamlete.[h] **3** Na mtu ye-
yote akiwaambia, ‘Kwa nini
mnafanya hili?’ semeni, ‘Bwa-
na anamhitaji, na atamrudisha
hapa mara moja.’”[i] **4** Kwa
hiyo wakaenda zao na ku-
mkuta mwana-punda akiwa
amefungwa kwenye mlango,
nje kwenye barabara ya ka-
ndokando, nao wakamfungua.[j]
5 Lakini baadhi ya wale wali-
okuwa wamesimama hapo wa-
kaanza kuwaambia: “Kwa nini
mnamfungua mwana-punda
huyu?”[k] **6** Wakawaambia
hao kama vile Yesu alivyoku-
wa amesema; nao wakawaacha
waende.[l]

7 Wakamletea Yesu huyo
mwana-punda,[m] nao wakawe-
ka mavazi yao ya nje juu
yake, naye akaketi juu yake.[n]
8 Pia, wengi wakatandaza ma-

SURA 10
a Mk 10:36
b Mt 20:33
Lu 18:41
c Mt 9:22
Lu 8:48
d Isa 35:5
Isa 42:7
Mk 8:25
Mdo 26:18
e Mt 20:34
Lu 18:43

SURA 11
f Yoh 11:18
g Mt 21:1
Lu 19:29
h Mt 21:2
Lu 19:30
i Mt 21:3
Lu 19:31
Yoh 13:13
j Mt 21:6
Lu 19:32
k Lu 19:33
l Lu 19:34
m 1Fa 1:33
Zek 9:9
n Mt 21:7
Yoh 12:14

Safu ya 2
a 2Fa 9:13
b Yoh 12:13
c Mt 21:8
Lu 19:36
d Zb 118:25
Mt 21:15
e Zb 118:26
Mt 21:9
Lu 19:38
Yoh 12:13
f Zek 9:9
Lu 1:32
Mdo 2:29
g Mt 21:10
h Mt 21:18
i Mt 21:19
j Mk 11:20
k Mt 21:12
Lu 19:45
Yoh 2:14

vazi[a] yao ya nje barabarani,
lakini wengine wakakata
matawi yenye majani[b] kuto-
ka katika mashamba.[c] **9** Na
wale waliokuwa wakitangu-
lia na wale waliokuwa waki-
fuata nyuma wakawa waki-
paaza sauti: “Mwokoe, tunao-
mba!![d] Aliyebarikiwa ni yule
anayekuja katika jina la Yeho-
va!![e] **10** Ufalme unaokuja wa
baba yetu Daudi[f] umebarikiwa!
Mwokoe, tunaomba, katika
vilele vilivyo juu!” **11** Naye
akaingia Yerusalemu, katika
hekalu; naye akatazama vitu
vyote huku na huku, na, kwa
kuwa saa ilikuwa tayari ime-
songa, akatoka kwenda Betha-
nia pamoja na wale kumi na
wawili.[g]

12 Siku iliyofuata, walipo-
kuwa wamekuja kutoka Be-
thania, akaona njaa.[h] **13** Na
kutoka mbali akaona mtini uli-
okuwa na majani, akaenda ku-
ona kama labda angeweza ku-
pata kitu fulani juu yake. La-
kini, alipofika mahali ulipoku-
wa, hakupata kitu ila majani,
kwa maana hayakuwa majira
ya tini.[i] **14** Kwa hiyo, akajibu
akauambia: “Mtu yeyote asile
matunda kutoka kwako tena
kamwe, milele.”[j] Nao wanafu-
nzi wake walikuwa wakisikili-
za.

15 Sasa wakafika Yerusa-
lemu. Huko akaingia katika
hekalu akaanza kuwafuku-
za wale waliokuwa wakiuza na
kununua katika hekalu, naye
akazipindua meza za wale wa-
liokuwa wakibadili pesa na
viti vya wale waliokuwa waki-
uza njiwa;[k] **16** naye hakuwa
akimruhusu mtu yeyote apiti-

she chombo hekaluni, **17** lakini akaendelea kufundisha na kusema: “Je, haikuandikwa, ‘Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala[a] kwa ajili ya mataifa yote’?[b] Lakini ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang’anyi.”[c] **18** Na wakuu wa makuhani na waandishi wakasikia, nao wakaanza kutafuta jinsi ya kumwangamiza;[d] kwa maana walikuwa wakimwogopa, kwa maana umati wote sikuzote ulikuwa ukistaajabishwa na mafundisho yake.[e]

19 Na ilipofika jioni, walikuwa wakitoka jijini. **20** Lakini walipokuwa wakipita hapo asubuhi na mapema, wakaona ule mtini tayari umekauka kuanzia kwenye mizizi.[f] **21** Kwa hiyo Petro, akakumbuka, akamwambia: “Rabi, ona! ule mtini ulioulaani umekauka.”[g] **22** Yesu akajibu, akawaambia: “Iweni na imani katika Mungu. **23** Kwa kweli ninawaambia ninyi kwamba mtu yeyote anayeuambia mlima huu, ‘Ng’oka ukatupwe baharini,’ naye hana shaka moyoni mwake lakini ana imani kwamba yale anayosema yatatukia, itakuwa hivyo kwake.[h] **24** Ndiyo sababu ninawaambia ninyi, Mambo yote mnayosali na kuomba juu yake iweni na imani kwamba ni kana kwamba tayari mmeyapokea, nanyi mtayapata.[i] **25** Na mnaposimama mkisali, wasameheni[j] watu chochote mlicho nacho dhidi yao; ili Baba yenu aliye mbinguni awasamehe makosa yenu ninyi pia.”[k] **26** ——

SURA 11

a 1Fa 8:43
Isa 56:7
b Isa 60:7
Zek 2:11
c Yer 7:11
Mt 21:13
Lu 19:46
Yoh 2:16
d Mk 14:1
Lu 19:47
Lu 20:19
e Mt 21:46
Lu 19:48
f Mt 21:19
g Mk 11:14
h Mt 17:20
Mt 21:21
Lu 17:6
1Ko 13:2
i Mt 7:7
Mt 18:19
Mt 21:22
Lu 11:9
Yoh 14:13
Yoh 15:7
Yoh 16:24
j Mt 6:14
Efe 4:32
Kol 3:13
k Zb 103:12
Mt 6:12

Safu ya 2

a Mt 21:23
Lu 20:1
b Lu 20:2
c Mt 21:24
Lu 20:3
d Mk 1:4
e Mt 21:25
Lu 20:4
f Lu 20:5
g Mt 3:5
Mt 14:5
Mt 21:26
Mk 6:20
Lu 20:6
h Met 26:4
Mt 7:6
Mt 21:27
Lu 20:8

SURA 12

i Zb 80:8
Yer 2:21
j Isa 5:2
k Wim 8:11
l Mt 21:33
Lu 20:9
m Mt 21:34
Lu 20:10

27 Nao wakaja tena Yerusalemu. Na alipokuwa akitembea katika hekalu, wakuu wa makuhani na waandishi na wanaume wazee wakamjia[a] **28** na kuanza kumwambia: “Unafanya mambo haya kwa mamlaka gani? au ni nani aliyekupa mamlaka ya kufanya mambo haya?”[b] **29** Yesu akawaambia: “Nitawauliza ninyi swali moja. Nijibuni, nami pia nitawaambia ninyi ninafanya mambo haya kwa mamlaka gani.[c] **30** Je, ubatizo[d] wa Yohana ulitoka mbinguni au kwa wanadamu? Nijibuni.”[e] **31** Kwa hiyo wakaanza kujadiliana kati yao wenyewe, wakisema: “Tukisema, ‘Ulitoka mbinguni,’ atasema, ‘Basi, kwa nini hamkumwamini?’[f] **32** Lakini je, tutathubutu kusema, ‘Ulitoka kwa wanadamu’?”—Walikuwa wakiuogopa umati, kwa maana umati wote huo ulimwona Yohana kwamba kwa kweli alikuwa nabii.[g] **33** Basi, wakamjibu Yesu wakasema: “Hatujui.” Naye Yesu akawaambia: “Wala mimi siwaambii ninyi ninafanya mambo haya kwa mamlaka gani.”[h]

12 Pia, akaanza kusema nao kwa kutumia mifano: “Mtu alipanda shamba la mizabibu,[i] akaweka ua kulizunguka, akachimba shimo la mtungi wa shinikizo la divai, akasimamisha mnara,[j] akalikodisha kwa wakulima,[k] kisha akasafiri kwenda ng’ambo.[l] **2** Majira yake yalipofika akatuma mtumwa kwa wakulima, ili apate sehemu ya matunda ya shamba la mizabibu kutoka kwa wakulima.[m] **3** Lakini

wakamchukua, wakampiga na
kumfukuza mikono mitupu.[a]
4 Na tena akamtuma mtumwa
mwingine kwao; na huyo wa-
kampiga kichwani na kumvu-
njia heshima.[b] **5** Naye aka-
mtuma mwingine, na huyo wa-
kamuua; na wengine wengi,
baadhi yao waliwapiga na ba-
adhi yao waliwaua. **6** Aliku-
wa na mmoja zaidi, mwana
mpendwa.[c] Akamtuma mwi-
sho kwao, akisema, 'Watamhe-
shimu mwanangu.'[d] **7** Laki-
ni wakulima hao wakasemeza-
na, 'Huyu ndiye mrithi.[e] Njo-
oni, acheni tumuue, na urithi
utakuwa wetu.'[f] **8** Kwa hiyo
wakamchukua wakamuua,[g] na
kumtupa nje ya shamba la mi-
zabibu.[h] **9** Mwenye shamba
la mizabibu atafanya nini? Ata-
kuja na kuwaangamiza waku-
lima, na kuwapa wengine[i] sha-
mba la mizabibu.[j] **10** Je, ha-
mkusoma kamwe andiko hili,
'Jiwe[k] ambalo wajenzi walili-
kataa, limekuwa jiwe kuu la
pembeni.[l] **11** Limetokana na
Yehova, nalo ni la kustaajabi-
sha machoni petu'?"[m]
12 Ndipo wakaanza kutafu-
ta jinsi ya kumkamata, lakini
waliuogopa umati, kwa maana
walijua kwamba alitoa mfano
huo juu yao. Kwa hiyo waka-
mwacha, wakaenda zao.[n]
13 Halafu wakamtumia ba-
adhi ya Mafarisayo na wafu-
asi wa chama cha Herode,[o]
kumnasa kwa maneno yake.[p]
14 Walipofika wakamwambia:
"Mwalimu, tunajua wewe una
ukweli nawe hujali mtu yeyote,
kwa maana hutazami
sura za watu, bali unafundi-
sha njia ya Mungu kupatana
na ile kweli:[q] Je, ni halali ku-

SURA 12

a Mt 21:35
b Mt 21:36
Lu 20:11
Ebr 11:37
c Zb 2:7
Mt 1:23
Ga 4:4
1Yo 4:9
d Mt 21:37
Lu 20:13
e Zb 2:8
Ebr 1:2
f Mt 21:38
Lu 20:14
g Mdo 2:23
h Mt 21:39
Lu 20:15
Ebr 13:12
i Mt 21:41
Lu 20:16
j Mdo 28:28
k Mdo 4:11
l Zb 118:22
Mt 21:42
Lu 20:17
Efe 2:20
1Pe 2:7
m Zb 118:23
n Mt 21:45
Mk 11:18
Lu 20:19
o Mk 3:6
p Mt 22:15
Lu 20:20
q Mt 22:16
Lu 20:21

Safu ya 2

a Mt 22:17
Lu 20:22
b Mt 22:18
Lu 20:23
c Mt 22:20
Lu 20:24
d Ro 13:7
Tit 3:1
1Pe 2:13
e Mt 22:21
Lu 20:25
f Mt 22:22
g Mt 22:23
Lu 20:27
Mdo 23:8
h Mwa 38:8
Kum 25:5
i Mt 22:24
Lu 20:28
j Mt 22:25
Lu 20:29
k Mt 22:26
Lu 20:31
l Mt 22:28
Lu 20:33
m Mt 22:29
Lu 20:34
n Mt 22:30
Lu 20:35

mlipa Kaisari kodi ya kichwa
au hapana? **15** Je, tulipe, au
tusilipe?"[a] Akagundua unafi-
ki wao, akawaambia: "Kwa
nini mnanijaribu? Nileteeni di-
nari niitazame."[b] **16** Wakale-
ta moja. Naye akawaambia:
"Sanamu hii na mwandiko huu
ni za nani?" Wakamwambia:
"Ni za Kaisari."[c] **17** Ndipo
Yesu akasema: "Mlipeni Kaisa-
ri vitu vya Kaisari,[d] lakini Mu-
ngu vitu vya Mungu."[e] Nao wa-
kaanza kumstaajabia.[f]
18 Sasa Masadukayo waka-
mjia, wale ambao husema ha-
kuna ufufuo, nao wakamuuliza:[g]
19 "Mwalimu, Musa ali-
tuandikia kwamba ndugu ya
mtu akifa na aache mke lakini
hakuacha mtoto, ndugu yake[h]
anapaswa kumchukua mke
huyo na kumwinulia ndugu
yake uzao kutoka kwa mwa-
namke huyo.[i] **20** Kulikuwa
na ndugu saba; na wa kwanza
akamchukua mke, lakini ali-
pokufa hakuacha uzao wowo-
te.[j] **21** Na yule wa pili aka-
mchukua, lakini akafa bila ku-
acha uzao; na yule wa tatu
vilevile. **22** Na wale saba ha-
wakuacha uzao wowote. Mwi-
showe yule mwanamke akafa
pia.[k] **23** Katika ufufuo ata-
kuwa mke wa nani kati yao?
Kwa sababu alikuwa mke wa
wale saba."[l] **24** Yesu akawaa-
mbia: "Je, hiyo siyo sababu ni-
nyi mmekosea, kutojua kwenu
Maandiko wala nguvu za Mu-
ngu?[m] **25** Kwa maana wana-
pofufuliwa kutoka kwa wafu,
wanaume hawaoi wala wana-
wake hawaolewi, bali wao ni
kama malaika wa mbinguni.[n]
26 Lakini kuhusu wafu, kwa-

mba wanafufuliwa, je, hamkusoma katika kitabu cha Musa,
katika masimulizi juu ya ule
mti wa miiba, jinsi Mungu ali-
vyomwambia, 'Mimi ni Mungu
wa Abrahamu na Mungu wa
Isaka na Mungu wa Yakobo'?[a]
27 Yeye ni Mungu, si wa wafu,
bali wa walio hai. Mmekosea
sana."[b]

28 Sasa mmoja kati ya wa-
andishi aliyekuwa amekuja na
kuwasikia wakibishana, akijua
kwamba alikuwa amewajibu
vizuri, akamuuliza: "Ni amri
gani iliyo ya kwanza kati ya
zote?"[c] **29** Yesu akajibu: "Ya
kwanza ni hii, 'Sikia, Ee Israe-
li, Yehova Mungu wetu ni Yeho-
va mmoja,[d] **30** nawe lazima
umpende Yehova Mungu wako
kwa moyo wako wote na kwa
nafsi yako yote na kwa akili
yako yote na kwa nguvu zako
zote.'[e] **31** Ya pili ni hii, 'Mpe-
nde jirani yako kama wewe
mwenyewe.'[f] Hakuna amri nyi-
ngine yoyote iliyo kubwa zai-
di kuliko hizi." **32** Yule mwa-
ndishi akamwambia: "Mwali-
mu, umesema vema kupatana
na kweli, 'Yeye ni Mmoja, na
hakuna mwingine ila Yeye';[g]
33 na jambo hili la mtu kum-
penda yeye kwa moyo wote
na kwa uelewaji wote na kwa
nguvu zote na mtu kumpe-
nda jirani kama yeye mwenye-
we ni bora zaidi kuliko matoleo
yote mazima ya kuteketezwa
na dhabihu zote."[h] **34** Ndipo
Yesu, akitambua kwamba ali-
kuwa amejibu kwa kutumia
akili, akamwambia: "Wewe
huko mbali na ufalme wa Mu-
ngu." Lakini hakuna mtu ali-
yekuwa tena na moyo wa ku-
muuliza swali.[i]

SURA 12

a Kut 3:2
Mt 22:31
Lu 20:37
b Mt 22:32
Lu 20:38
c Mt 22:35
d Kum 6:4
e Kum 6:5
Yos 22:5
Mt 22:37
Lu 10:27
f Law 19:18
Mt 22:39
Ro 13:9
Ga 5:14
Yak 2:8
g Kum 4:39
Kum 6:4
Isa 45:21
Isa 46:9
1Ko 8:4
h Kum 6:5
1Sa 15:22
Ho 6:6
Mik 6:6
i Mt 22:46

Safu ya 2

a Mt 22:42
Lu 20:41
Yoh 7:42
b 2Sa 23:2
2Ti 3:16
2Pe 1:21
c Zb 110:1
Mt 22:44
Mdo 2:34
1Ko 15:25
Ebr 1:13
d Ro 1:3
Ufu 22:16
e Lu 19:48
Lu 21:38
f Mt 23:1
Lu 20:46
g Mt 23:6
Lu 11:43
Lu 20:46
h 2Ti 3:6
i Mt 23:14
j 2Fa 12:9
Yoh 8:20
k Lu 21:1
l Lu 21:2

35 Hata hivyo, alipokuwa
akijibu, Yesu akaanza kuse-
ma akifundisha katika hekalu:
"Kwa nini waandishi husema
kwamba Kristo ni mwana wa
Daudi?[a] **36** Kwa roho takati-
fu[b] Daudi mwenyewe alisema,
'Yehova alimwambia Bwana
wangu: "Keti kwenye mkono
wangu wa kuume mpaka niwa-
weke adui zako chini ya mi-
guu yako."'[c] **37** Daudi mwe-
nyewe anamwita 'Bwana,' la-
kini inawezekanaje kwamba
yeye ni mwana wake?"[d]

Na umati mkubwa ulikuwa
ukimsikiliza kwa furaha.[e]
38 Na katika mafundisho yake
akaendelea kusema: "Jihadha-
rini na waandishi[f] ambao hu-
penda kutembea wakiwa wa-
mevaa kanzu na hupenda sala-
mu katika masoko **39** na viti
vya mbele katika masinagogi
na mahali penye kuonekana
zaidi kwenye milo ya jioni.[g]
40 Wao ndio wanaomeza nyu-
mba[h] za wajane na kutoa sala
ndefu kwa kisingizio; hawa wa-
tapokea hukumu nzito zaidi."[i]

41 Naye akaketi akitazama
masanduku ya hazina[j] na ku-
anza kuangalia jinsi umati uli-
vyokuwa ukitumbukiza pesa
ndani ya masanduku hayo; na
matajiri wengi walikuwa wa-
kitumbukiza ndani sarafu nyi-
ngi.[k] **42** Sasa mjane fulani
maskini akaja, akatumbuki-
za ndani sarafu mbili ndogo,
zenye thamani ndogo sana.[l]
43 Kwa hiyo akawaita wana-
funzi wake na kuwaambia:
"Kwa kweli ninawaambia kwa-
mba mjane huyu maskini ame-
tumbukiza nyingi kuliko wote
waliokuwa wakitumbukiza
pesa ndani ya masanduku ya

hazina;[a] **44** kwa sababu wote
walitumbukiza ndani kutoka-
na na ziada yao, lakini yeye,
kutokana na uhitaji wake, ali-
tumbukiza ndani vyote alivyo-
kuwa navyo, riziki yake yote."[b]

13 Alipokuwa akitoka he-
kaluni mmoja wa wa-
nafunzi wake akamwambia:
"Mwalimu, ona! jinsi yalivyo
mawe haya na majengo haya!"[c]
2 Hata hivyo, Yesu aka-
mwambia: "Unayaona maje-
ngo haya makubwa?[d] Hakuna
jiwe litakaloachwa hapa juu ya
jiwe[e] nalo lisiangushwe chini."[f]
3 Na alipokuwa ameketi juu
ya Mlima wa Mizeituni, hekalu
likiwa linaonekana, Petro[g] na
Yakobo na Yohana na Andrea
wakaanza kumuuliza fara-
ghani:[h] **4** "Tuambie, mambo
haya yatakuwa wakati gani,
na ni nini itakayokuwa ishara
ya wakati ambapo mambo yote
haya yanakusudiwa kufikia
mwisho?"[i] **5** Kwa hiyo Yesu
akaanza kuwaambia: "Jiha-
dharini mtu yeyote asiwapoto-
she.[j] **6** Wengi watakuja kwa
msingi wa jina langu, wakise-
ma, 'Mimi ndiye,' nao watawa-
potosha wengi.[k] **7** Zaidi ya
hayo, mnaposikia juu ya vita
na habari za vita, msiogope;
mambo hayo lazima yatukie,
lakini ule mwisho bado.[l]
8 "Kwa maana taifa litasi-
mama kupigana na taifa na
ufalme kupigana na ufalme,[m]
kutakuwa na matetemeko ya
nchi[n] mahali pamoja baada ya
pengine, kutakuwa na upu-
ngufu wa chakula.[o] Hayo ni
mwanzo wa maumivu ya ta-
abu.[p]
9 "Kwa habari yenu, jiha-
dharini; watu watawapeleka
mahakamani,[a] nanyi mtapigwa
katika masinagogi[b] na kusi-
mamishwa mbele ya maga-
vana na wafalme kwa ajili
yangu, kuwa ushahidi kwao.[c]
10 Pia, katika mataifa yote la-
zima habari njema[d] ihubiriwe
kwanza.[e] **11** Lakini wanapo-
wapeleka, msihangaike kimbe-
le juu ya jambo mtakalosema;[f]
bali jambo lolote mtakalope-
wa saa hiyo, semeni hilo, kwa
maana si ninyi mnaosema, bali
ni roho takatifu.[g] **12** Zaidi
ya hayo, ndugu atamtoa ndu-
gu yake auawe, na baba ata-
mtoa mtoto,[h] na watoto watai-
nuka juu ya wazazi na kufa-
nya wauawe;[i] **13** nanyi mta-
chukiwa na watu wote kwa
sababu ya jina langu.[j] Lakini
yule ambaye atavumilia mpa-
ka mwisho[k] ndiye atakayeoko-
lewa.[l]
14 "Hata hivyo, mtakapoo-
na lile chukizo[m] linalosaba-
bisha ukiwa likiwa[n] limesima-
ma mahali ambapo halipaswi
(msomaji na atumie utambu-
zi),[o] ndipo wale walio katika
Yudea waanze kukimbilia mi-
limani.[p] **15** Mtu aliye juu ya
paa ya nyumba asishuke, wala
asiingie ndani kuchukua kitu
chochote kutoka nyumbani
mwake;[q] **16** na mtu aliye
shambani asirudi kwenye vitu
vilivyo nyuma kuchukua vazi
lake la nje.[r] **17** Ole wao wa-
nawake wenye mimba na
wale wanaonyonyesha mtoto
mchanga katika siku hizo![s]
18 Endeleeni kusali kwamba
yasitukie wakati wa majira
ya baridi kali;[t] **19** kwa maa-
na siku hizo zitakuwa siku

SURA 12
a 1Nya 29:9
Lu 21:3
2Ko 8:12
b 1Nya 29:9
Lu 21:4

SURA 13
c Mt 24:1
Lu 21:5
d Yer 7:14
e Lu 19:44
f Law 26:31
Mt 24:2
Lu 21:6
g Mt 17:1
h Mt 24:3
i Lu 21:7
j Yer 29:8
Mt 24:4
k Mt 24:5
Lu 21:8
l Mt 24:6
m Lu 21:10
Ufu 6:4
n Mt 24:7
o Lu 21:11
Ufu 6:6
Ufu 6:8
p Mt 24:8

Safu ya 2
a Mdo 4:15
b Mt 10:17
Lu 21:12
Yoh 16:2
Ufu 2:10
c Mt 24:9
Lu 21:12
2Ti 3:12
d Mdo 8:12
e Mt 24:14
Ro 10:18
Ufu 14:6
f Mt 10:19
Lu 12:11
Lu 21:14
g Kut 4:12
Lu 21:15
Mdo 4:8
Mdo 6:10
h Mik 7:6
Mt 10:21
Lu 21:16
2Ti 3:3
i Mt 24:10
2Ti 3:1
j Lu 21:17
k Da 12:12
2Ti 4:7
Ebr 3:6
l Ufu 2:10
m Kum 29:17
1Fa 11:5
Ufu 13:15
n Da 9:27
o Mt 24:15
p Mt 24:16
q Mt 24:17
r Mt 24:18
s Mt 24:19
Lu 19:44
Lu 21:23
Lu 23:28
t Mt 24:20

za dhiki[a] ya namna ambayo
haijatukia tangu mwanzo wa
uumbaji ambao Mungu aliu-
mba mpaka wakati huo, na hai-
tatukia tena.[b] **20** Kwa kweli,
kama Yehova[c] hangezifupisha
siku hizo, hakuna chochote
chenye mwili ambacho kinge-
okolewa. Lakini amezifupisha
siku hizo[d] kwa sababu ya walio-
chaguliwa[e] ambao amewacha-
gua.[f]
21 "Ndipo, pia, mtu yeyote
akiwaambia, 'Tazameni! Kri-
sto huyu hapa,' 'Tazameni! ndi-
ye yule pale,'[g] msiamini.[h]
22 Kwa maana Makristo wa
uwongo na manabii wa uwo-
ngo watatokea[i] na kutoa ishara
na maajabu[j] ili kupotosha,
ikiwezekana, wale waliochagu-
liwa.[k] **23** Basi, jihadharini;[l]
nimewaambia mambo yote ki-
mbele.[m]
24 "Lakini katika siku hizo,
baada ya dhiki hiyo, jua lita-
tiwa giza, na mwezi hautatoa
nuru yake, **25** nazo nyota zi-
takuwa zikianguka kutoka
mbinguni na nguvu zilizo mbi-
nguni zitatikiswa.[n] **26** Ndipo
watakapomwona Mwana wa
binadamu[o] akija katika mawi-
ngu akiwa na nguvu nyingi na
utukufu.[p] **27** Ndipo atakapo-
watuma malaika na kuwaku-
sanya pamoja watu wake wa-
liochaguliwa[q] kutoka zile pepo
nne, kutoka mwisho wa dunia
mpaka mwisho wa mbingu.[r]
28 "Basi kutokana na mti-
ni jifunzeni mfano huu: Mara
tu tawi lake changa linapo-
kuwa jororo na kutoa maja-
ni yake, mnajua kwamba ki-
angazi kiko karibu.[s] **29** Vi-
vyo hivyo ninyi pia, mnapo-
ona mambo hayo yakitukia,

SURA 13
a Da 12:1 Yoe 2:2 Ufu 7:14
b Mt 24:21
c Isa 1:9 Zek 13:8
d Mt 24:22
e Ufu 17:14
f Ro 8:33 Efe 1:4
g Lu 17:23 Lu 21:8
h Mt 24:23 1Yo 4:1
i Kum 13:1 Kum 18:22 Mt 7:15
j Ufu 13:13
k Mt 24:24
l Mt 7:15 Mt 24:42 Efe 6:18 2Pe 3:17
m Yoh 13:19
n Mt 24:29
o Da 7:13 Mdo 1:11 Ufu 1:7
p Mt 24:30 Lu 21:27
q Ufu 7:3
r Kum 30:4 Zek 2:6 Mt 24:31
s Mt 24:32 Lu 21:29

Safu ya 2
a Mt 24:33 Mk 13:28
b Mt 24:34 Lu 21:32
c Zb 102:26 Isa 51:6
d Yos 23:14 Isa 40:8
e Mt 5:18 Mt 24:35 Lu 16:17
f Mt 24:36 Mdo 1:7
g Ro 13:11 1Th 5:6
h Mt 25:13 Lu 21:34
i Mt 25:14
j Mt 24:42 Lu 12:36 Mdo 20:31 Ufu 3:3
k Lu 12:38 Lu 21:36
l Mt 25:5
m Hab 2:3

SURA 14
n Kut 12:6 Law 23:5 Lu 22:1 Yoh 13:1
o Law 23:6
p Mt 26:2
q Mt 26:4 Lu 22:2
r Mt 26:5
s Mt 26:6

jueni kwamba yuko karibu, mi-
langoni.[a] **30** Kwa kweli nina-
waambia ninyi kwamba kizazi
hiki hakitapitilia mbali kamwe
mpaka mambo yote hayo yatu-
kie.[b] **31** Mbingu[c] na dunia zi-
tapitilia mbali, lakini maneno[d]
yangu hayatapitilia mbali.[e]
32 "Kuhusu siku ile au saa
ile hakuna mtu anayejua, wala
malaika mbinguni wala Mwa-
na, ila Baba.[f] **33** Endeleeni
kutazama, Endeleeni kuke-
sha,[g] kwa maana hamjui waka-
ti uliowekwa ni gani.[h] **34** Ni
kama mtu anayesafiri kwenda
ng'ambo,[i] ambaye aliacha nyu-
mba yake na kuwapa mamla-
ka watumwa wake, kila mmoja
kazi yake, na kumwamuru
mtunza-mlango aendelee ku-
kesha. **35** Kwa hiyo endele-
eni kukesha,[j] kwa maana ha-
mjui bwana wa nyumba anaku-
ja wakati gani, kama ni wa-
kati wa jioni au katikati ya
usiku au anapowika jogoo au
asubuhi na mapema;[k] **36** ili
anapofika kwa ghafula, asiwa-
kute mkiwa mmelala usingi-
zi.[l] **37** Lakini lile ninalowaa-
mbia ninyi ninawaambia wote,
Endeleeni kukesha."[m]

14 Siku mbili kabla ya pasa-
ka[n] na sherehe[o] ya keki
zisizo na chachu,[p] wakuu wa
makuhani na waandishi wali-
kuwa wakitafuta jinsi ya ku-
mkamata kwa hila na kumu-
ua;[q] **2** kwa maana walisema
tena na tena: "Si kwenye shere-
he; huenda kukawa na ghasia
ya watu."[r]
3 Na alipokuwa Bethania
katika nyumba ya Simoni
mwenye ukoma,[s] akiwa ame-
keti kwenye mlo, mwanamke

akaja na chupa ya alabasta iliyo na mafuta yenye marashi,
nardo halisi, ghali sana. Akaivunja ili kuifungua na kuanza kuyamimina juu ya kichwa chake.[a] **4** Ndipo wengine wakakasirika na kusema katikati yao wenyewe: "Kwa nini hasara hii ya mafuta yenye marashi?[b] **5** Kwa maana mafuta hayo yangaliweza kuuzwa kwa dinari zaidi ya mia tatu na kupewa maskini!" Nao walikuwa wamechukizwa sana na mwanamke huyo.[c] **6** Lakini Yesu akasema: "Mwacheni. Kwa nini mnataka kumsumbua? Amenifanyia tendo zuri.[d] **7** Kwa maana mna maskini[e] pamoja nanyi sikuzote, na wakati wowote ule mnapotaka mnaweza kuwafanyia mema sikuzote, lakini mimi hamtakuwa pamoja nami sikuzote.[f] **8** Alifanya jambo ambalo aliweza; ameutia mwili wangu mafuta yenye marashi ili kunitayarisha kimbele kwa ajili ya maziko yangu.[g] **9** Kwa kweli ninawaambia ninyi, Kokote ambako habari njema itahubiriwa katika ulimwengu wote,[h] jambo ambalo mwanamke huyu amefanya litasimuliwa pia kuwa kumbukumbu lake."[i]

10 Na Yuda Iskariote, mmoja wa wale kumi na wawili, akaenda zake kwa wakuu wa makuhani ili amsaliti kwao.[j] **11** Waliposikia hilo, wakashangilia na kuahidi kumpa fedha.[k] Kwa hiyo akaanza kutafuta jinsi ya kumsaliti kwa wakati unaofaa.[l]

12 Sasa siku ya kwanza ya keki zisizo na chachu,[m] wakati ambapo kidesturi walichinja mnyama wa pasaka, wanafunzi[a] wake wakamwambia: "Unataka twende wapi tukakutayarishie ule pasaka?"[b] **13** Ndipo akawatuma wawili kati ya wanafunzi wake na kuwaambia: "Nendeni jijini, nanyi mtakutana na mwanamume anayebeba chombo cha udongo cha maji.[c] Mfuateni, **14** na popote atakapoingia mwambieni mwenye nyumba, 'Mwalimu anasema: "Kiko wapi chumba cha wageni kwa ajili yangu ambamo ninaweza kula pasaka[d] pamoja na wanafunzi wangu?"'[e] **15** Naye atawaonyesha chumba kikubwa cha juu, chenye vifaa kikiwa tayari; na humo tayarisheni kwa ajili yetu."[f] **16** Kwa hiyo wanafunzi wakaenda, nao wakaingia katika jiji na kukipata kama vile alivyowaambia; nao wakafanya matayarisho ya pasaka.[g]

17 Baada ya kuwa jioni akaja pamoja na wale kumi na wawili.[h] **18** Na walipokuwa wameketi mezani wakila, Yesu akasema: "Kwa kweli ninawaambia ninyi, Mmoja wenu, anayekula[i] pamoja nami, atanisaliti."[j] **19** Wakaanza kuhuzunika na kumwambia mmoja-mmoja; "Je, ni mimi?"[k] **20** Akawaambia: "Ni mmoja wa wale kumi na wawili, anayechovya pamoja nami katika bakuli moja.[l] **21** Kwa kweli, Mwana wa binadamu anaenda zake, kama ilivyoandikwa kumhusu, lakini ole wake mtu yule ambaye kupitia kwake Mwana wa binadamu atasalitiwa! Ingalikuwa afadhali kama mtu huyo asingalizaliwa."[m]

SURA 14

a Mt 26:7
Yoh 12:3
b Mt 26:8
Yoh 12:4
c Mt 26:9
Yoh 12:5
d Mt 26:10
Yoh 12:7
e Kum 15:11
Yoh 12:8
f Mt 26:11
Yoh 12:8
g Mt 26:12
h Mt 24:14
i Mt 26:13
j Mt 26:14
Lu 22:4
k Kum 27:25
Zek 11:12
Mt 26:15
Lu 22:5
1Ti 6:10
l Mt 26:16
Lu 22:6
m Kut 12:15
Kut 12:18
Kut 23:15
Law 23:6
Lu 22:7

Safu ya 2

a Lu 22:8
b Hes 9:2
Mt 26:17
Lu 22:9
c Mt 26:18
Lu 22:10
d Kut 12:6
Law 23:5
e Lu 22:11
f Lu 22:12
g Mt 26:19
Lu 22:13
h Mt 26:20
Lu 22:14
i Zb 41:9
j Mt 26:21
Lu 22:21
Yoh 13:21
k Mt 26:22
Lu 22:23
Yoh 13:22
l Mt 26:23
m Ayu 3:3
Mt 26:24

22 Na walipokuwa wakiendelea kula, akachukua mkate, akatoa baraka, akaumega, akawapa, na kusema: "Chukueni, huu unamaanisha mwili wangu."[a] **23** Naye akichukua kikombe, akashukuru akawapa, nao wote wakakinywea.[b] **24** Naye akawaambia: "Hii inamaanisha 'damu[c] yangu ya agano,'[d] ambayo itamwagwa[e] kwa ajili ya wengi.[f] **25** Kwa kweli ninawaambia ninyi, Sitakunywa tena kamwe divai ya mzabibu mpaka siku ile nitakapokunywa ikiwa mpya katika ufalme wa Mungu."[g] **26** Mwishowe, baada ya kuimba sifa,[h] wakatoka na kwenda kwenye Mlima wa Mizeituni.[i]

27 Na Yesu akawaambia: "Ninyi nyote mtakwazika, kwa sababu imeandikwa, 'Nitampiga mchungaji,[j] nao kondoo watatawanyika huku na huku.'[k] **28** Lakini baada ya kufufuliwa nitawatangulia kuingia Galilaya."[l] **29** Lakini Petro akamwambia: "Hata ikiwa wengine wote watakwazika, hata hivyo mimi sitakwazika."[m] **30** Ndipo Yesu akamwambia: "Kwa kweli ninakuambia, Wewe leo, ndiyo, usiku huu, kabla ya jogoo kuwika mara mbili, utanikana mara tatu."[n] **31** Lakini akaanza kusema maneno kwa kusisitiza: "Nikilazimika kufa pamoja nawe, sitakukana kamwe." Pia, wengine wote wakaanza kusema vivyo hivyo.[o]

32 Kwa hiyo wakafika mahali panapoitwa jina Gethsemane, naye akawaambia wanafunzi wake: "Ketini hapa ninaposali."[a] **33** Akamchukua Petro na Yakobo na Yohana[b] pamoja naye, naye akaanza kufadhaika na kutaabika sana.[c] **34** Kisha akawaambia: "Nafsi yangu ina huzuni sana,[d] kiasi cha kufa. Kaeni hapa na mwendelee kukesha."[e] **35** Naye akasonga mbele kidogo, akaanguka chini na kuanza kusali kwamba, kama ingewezekana, saa hiyo ipite mbali kutoka kwake.[f] **36** Naye akaendelea kusema: *"Abba,* Baba,[g] mambo yote yanawezekana kwako; niondolee kikombe hiki. Lakini si lile ninalotaka, bali lile unalotaka."[h] **37** Naye akaja akawakuta wamelala usingizi, naye akamwambia Petro: "Simoni, unalala usingizi? Hukuwa na nguvu za kuendelea kukesha kwa saa moja?[i] **38** Endeleeni kukesha na kusali,[j] ili msiingie katika jaribu. Bila shaka, roho inataka, lakini mwili ni dhaifu."[k] **39** Naye akaenda zake tena, akasali, akisema neno hilohilo.[l] **40** Akaja tena na kuwakuta wamelala usingizi, kwa maana macho yao yalikuwa yamelemewa, na kwa hiyo hawakujua wamjibu nini.[m] **41** Naye akaja mara ya tatu na kuwaambia: "Wakati kama huu ninyi mnalala usingizi na kupumzika! Inatosha! Saa imekuja![n] Tazama! Mwana wa binadamu anasalitiwa na kutiwa katika mikono ya watenda-dhambi.[o] **42** Simameni, twende.[p] Tazama! Msaliti wangu amekaribia."[q]

43 Na mara moja, alipokuwa bado akisema, Yuda, mmoja wa wale kumi na wawili, akafika pamoja na umati ukiwa

SURA 14

a Mt 26:26
Lu 22:19
1Ko 10:16
1Ko 11:24
b Mt 26:27
Yoh 6:53
1Ko 10:16
1Ko 11:25
c Kut 24:8
Law 17:11
Zek 9:11
Ebr 9:22
d Yer 31:31
Ebr 7:22
Ebr 9:15
e Isa 53:12
f Mt 26:28
Lu 22:20
g 1Ko 11:26
h Zb 113:1-9
i Mt 26:30
Lu 22:39
Yoh 18:1
j Isa 53:5
Da 9:26
Zek 13:7
k Mt 26:31
Mt 26:56
Mk 14:50
Yoh 16:32
l Mt 26:32
Mk 16:7
m Met 11:2
Mt 26:33
Lu 22:33
Yoh 13:37
n Mt 26:34
Lu 22:34
Yoh 13:38
o Mt 26:35

Safu ya 2

a Mt 26:36
Lu 22:39
Yoh 18:1
b Mt 17:1
c Mt 26:37
d Zb 42:5
Zb 43:5
Yoh 12:27
e Mt 26:38
f Mt 26:39
Lu 22:41
g Ro 8:15
Ga 4:6
h Lu 22:42
Yoh 6:38
Ebr 5:7
i Mt 26:40
Lu 22:45
j Mt 6:13
Lu 11:4
k Mt 26:41
Ro 7:23
Ga 5:17
l Mt 26:42
m Mt 26:43
n Yoh 13:1
o Mt 26:45
p Yoh 14:31
q Mt 26:46
Yoh 18:2

na mapanga na marungu kutoka kwa wakuu wa makuhani na waandishi na wanaume wazee.[a] **44** Basi msaliti wake alikuwa amewapa ishara waliyokubaliana, akisema: "Yeyote yule nitakayembusu, huyo ndiye; mkamateni na kumchukua."[b] **45** Naye akaja moja kwa moja akamkaribia na kusema: "Rabi!" na kumbusu[c] kwa wororo sana. **46** Kwa hiyo wakaweka mikono juu yake wakamkamata.[d] **47** Hata hivyo, mtu fulani kati ya hao waliosimama kando akauchomoa upanga wake, akampiga mtumwa wa kuhani mkuu, akalikata sikio lake.[e] **48** Lakini Yesu akawaambia: "Je, mlitoka mkiwa na mapanga na marungu kana kwamba ni kwenda juu ya mnyang'anyi ili kunikamata?[f] **49** Nilikuwa pamoja nanyi katika hekalu siku baada ya siku nikifundisha,[g] na bado hamkunikamata. Hata hivyo, ni ili Maandiko[h] yapate kutimizwa."[i]

50 Nao wote wakamwacha[j] na kukimbia.[k] **51** Lakini kijana fulani aliyekuwa amevaa vazi la kitani bora juu ya mwili wake ulio uchi akaanza kumfuata karibu-karibu; nao wakajaribu kumkamata,[l] **52** lakini yeye akaliacha vazi lake la kitani, akakimbia akiwa uchi.

53 Sasa wakampeleka Yesu kwa kuhani mkuu, na wakuu wote wa makuhani na wanaume wazee na waandishi wakakusanyika.[m] **54** Lakini Petro, akiwa mbali kiasi, akamfuata[n] mpaka katika ua wa kuhani mkuu; naye alikuwa ameketi pamoja na watumishi wa nyumba akiota moto, mbele ya moto mwangavu. **55** Wakati huohuo wakuu wa makuhani na Sanhedrini yote walikuwa wakitafuta ushuhuda juu ya Yesu ili auawe,[a] lakini hawakuwa wakipata wowote.[b] **56** Kwa kweli, wengi walikuwa wakitoa ushahidi wa uwongo juu yake,[c] lakini ushuhuda wao haukupatana.[d] **57** Pia, watu fulani walikuwa wakisimama na kutoa ushahidi wa uwongo juu yake, wakisema: **58** "Sisi tulimsikia akisema, 'Nitaliangusha hekalu hili lililotengenezwa kwa mikono na katika siku tatu nitajenga lingine lisilotengenezwa kwa mikono.'"[e] **59** Lakini hata kwa misingi hiyo ushuhuda wao haukupatana.

60 Mwishowe kuhani mkuu akasimama katikati yao na kumuuliza Yesu, akisema: "Je, hujibu lolote? Watu hawa wanashuhudia nini juu yako?"[f] **61** Lakini akaendelea kukaa kimya na hakutoa jibu hata kidogo.[g] Tena kuhani mkuu akaanza kumuuliza na kumwambia: "Wewe ndiye Kristo Mwana wa yule Mbarikiwa?"[h] **62** Ndipo Yesu akasema: "Mimi ndiye; nanyi mtamwona Mwana wa binadamu[i] akiwa ameketi kwenye mkono wa kuume[j] wa nguvu akija pamoja na mawingu ya mbinguni."[k] **63** Ndipo kuhani mkuu akayararua mavazi yake ya ndani[l] na kusema: "Tunahitaji mashahidi wengine wa nini?[m] **64** Mmelisikia kufuru.[n] Ni jambo gani lililo wazi kwenu?" Wao wote wakamhukumu kwamba anastahili

SURA 14

a Mt 26:47
Lu 22:47
Yoh 18:3
b Mt 26:48
c 2Sa 20:9
d Mt 26:50
Lu 22:49
e Mt 26:51
Lu 22:50
Yoh 18:10
f Mt 26:55
Lu 22:52
g Lu 19:47
Yoh 18:20
h Zb 22:6
Isa 53:7
Da 9:26
Lu 22:37
i Mt 26:56
Ufu 19:10
j Zb 38:11
Zb 88:8
2Ti 4:16
k Zek 13:7
Mt 26:31
Yoh 16:32
l Yoh 18:15
m Mt 26:57
Lu 22:54
Yoh 18:13
n Mt 26:58
Yoh 18:15

Safu ya 2

a Zb 37:12
Zb 37:32
b Da 6:4
Mt 26:59
1Pe 3:16
c Kut 20:16
Kum 19:16
Zb 35:11
Met 19:5
d Mt 26:60
e Mt 26:61
Mk 15:29
Yoh 2:19
f Mt 26:62
g Isa 53:7
1Pe 2:23
h Mt 26:63
i Da 7:13
Mt 24:30
j Zb 110:1
Efe 1:20
Kol 3:1
k Mt 26:64
Lu 21:27
Ufu 1:7
Ufu 14:14
l Law 10:6
m Mt 26:65
n Law 24:16
1Fa 21:13
Yoh 19:7

kufa. **65** Na wengine wakaanza kumtemea mate[a] na kuufunika uso wake wote na kumpiga ngumi na kumwambia: "Toa unabii!" Na, wakimpiga makofi usoni, watumishi wa mahakama wakamchukua.[b]

66 Sasa Petro alipokuwa chini katika ua, mmoja wa vijakazi wa kuhani mkuu akaja,[c] **67** na, alipomwona Petro akiota moto, akamtazama moja kwa moja na kusema: "Wewe, pia, ulikuwa pamoja na yule Mnazareti, Yesu huyu."[d] **68** Lakini akakana, akisema: "Simjui wala sielewi unalosema," naye akaenda nje kwenye sebule.[e] **69** Huko yule kijakazi, alipomwona, akaanza tena kuwaambia wale waliosimama kando: "Huyu ni mmoja wao."[f] **70** Tena akawa akikana hilo. Na mara nyingine tena baada ya muda kidogo wale waliosimama kando wakaanza kumwambia Petro: "Hakika wewe ni mmoja wao, kwa maana, kwa kweli, wewe ni Mgalilaya."[g] **71** Lakini yeye akaanza kulaani na kuapa:[h] "Simjui mtu huyu ambaye mnasema juu yake."[i] **72** Na mara jogoo akawika mara ya pili;[j] na Petro akakumbuka maneno ambayo Yesu alimwambia: "Kabla ya jogoo kuwika mara mbili, utanikana mara tatu."[k] Naye akaanza kulia.[l]

15 Na mara tu kulipopambazuka wakuu wa makuhani pamoja na wanaume wazee na waandishi, hata Sanhedrini yote, wakashauriana,[m] nao wakamfunga Yesu, wakampeleka na kumtia mikononi mwa Pilato.[n] **2** Kwa hiyo Pilato akamuuliza: "Je, wewe ndiye mfalme wa Wayahudi?"[a] Akamjibu, akasema: "Wewe mwenyewe unasema."[b] **3** Lakini wakuu wa makuhani wakaendelea kumshtaki mambo mengi.[c] **4** Sasa Pilato akaanza kumuuliza tena, akisema: "Je, huna jibu la kutoa?[d] Ona ni mashtaka mangapi wanaleta juu yako."[e] **5** Lakini Yesu hakujibu tena, hivi kwamba Pilato akaanza kustaajabu.[f]

6 Basi, kutoka sherehe mpaka sherehe alikuwa na kawaida ya kuwafungulia mfungwa mmoja, ambaye waliomba.[g] **7** Wakati huo yule aliyeitwa Baraba alikuwa amefungwa pamoja na wachochezi, ambao katika uchochezi wao walikuwa wameua.[h] **8** Kwa hiyo umati ukaja na kuanza kuomba kulingana na jambo alilokuwa na kawaida ya kuwafanyia. **9** Pilato akawajibu, akisema: "Mnataka niwafungulie mfalme wa Wayahudi?"[i] **10** Kwa maana alijua kwamba wakuu wa makuhani walikuwa wamemtia mikononi mwake[j] kwa sababu ya wivu.[k] **11** Lakini wakuu wa makuhani wakauchochea umati ili umfanye awafungulie Baraba, badala yake.[l] **12** Pilato akajibu tena, akawaambia: "Basi, nitafanya nini na huyu mnayemwita mfalme[m] wa Wayahudi?"[n] **13** Mara nyingine tena wakapaaza sauti: "Mtundike mtini!"[o] **14** Lakini Pilato akaendelea kuwaambia: "Kwani, alifanya jambo gani baya?" Bado wao wakapaaza sauti hata zaidi: "Mtundike mtini!"[p] **15** Ndipo Pilato, akitaka kuuridhisha umati,[q] akawafungulia Baraba, na, baada ya kuagiza

SURA 14

a Isa 50:6; Isa 53:3; Mt 26:67
b Lu 22:64
c Mt 26:69; Lu 22:55; Yoh 18:18
d Lu 22:56
e Mt 26:70; Lu 22:57
f Mt 26:71; Lu 22:58; Yoh 18:25
g Mt 26:73; Lu 22:59; Yoh 18:26
h Met 29:25; Mt 5:37
i Mt 26:74
j Lu 22:61; Yoh 18:27
k Mt 26:34; Mk 14:30; Lu 22:34; Yoh 13:38
l 2Ko 7:10

SURA 15

m Zb 2:2; Mdo 4:26
n Mt 27:1; Lu 22:66; Yoh 18:28; Mdo 3:13

Safu ya 2

a Zb 2:2; Yoh 18:33
b Mt 27:11; Lu 23:3
c Mt 27:12
d Mt 26:62
e Mt 27:13; Yoh 19:10
f Isa 53:7; Mt 27:14; Yoh 19:9
g Mt 27:15; Lu 23:17; Yoh 18:39
h Mt 27:16
i Mt 27:17; Lu 23:16
j Mt 27:18
k Met 27:4; Mt 21:38; Mdo 13:45
l Mt 27:20; Mdo 3:14
m Zb 2:6; Isa 9:6; Yer 23:5
n Mt 27:22; Lu 23:20
o Lu 23:21; Yoh 19:6
p Mt 27:23; Lu 23:22; Mdo 3:13; Mdo 13:28
q Met 29:25

Yesu apigwe mijeledi, akamtoa
ili atundikwe mtini.[a]
16 Sasa askari-jeshi wakam-
peleka uani, yaani, katika ju-
mba la gavana; nao wakaita ki-
kosi chote cha askari pamoja,[b]
17 nao wakampamba kwa vazi
la zambarau na kusokota taji
la miiba, wakaliweka juu yake.[c]
18 Nao wakaanza kumsalimu:
"Siku njema,[d] ewe Mfalme wa
Wayahudi!" **19** Pia, wakawa
wakimpiga kichwani kwa ute-
te na kumtemea mate na ku-
msujudia wakiwa wamepiga
magoti.[e] **20** Mwishowe, wali-
pokuwa wamemdhihaki, wa-
kamvua lile vazi la zamba-
rau na kumvika mavazi yake
ya nje. Nao wakamtoa ili wa-
kamtundike mtini.[f] **21** Pia,
wakamlazimisha mpita-njia
afanye utumishi, mtu fulani
anayeitwa Simoni, wa Kirene,
aliyekuwa akija kutoka ma-
shambani, baba ya Aleksanda
na Rufo, kwamba aubebe mti
wake wa mateso.[g]
22 Kwa hiyo wakampeleka
mahali panapoitwa *Golgotha,*
neno ambalo linapotafsiriwa
humaanisha, Mahali pa Fuvu
la Kichwa.[h] **23** Hapa wakaja-
ribu kumpa divai iliyotiwa ki-
leo cha manemane,[i] lakini ha-
kuinywa.[j] **24** Nao wakamtu-
ndika mtini na kugawa ma-
vazi yake ya nje[k] kwa kupiga
kura juu yake kuhusu nani
achukue nini.[l] **25** Sasa iliku-
wa saa tatu,[m] nao wakamtundi-
ka mtini. **26** Na maandishi
ya shtaka[n] juu yake yakaandi-
kwa, "Mfalme wa Wayahu-
di."[o] **27** Zaidi ya hayo, waka-
watundika mtini wanyang'a-
nyi wawili pamoja naye, mmo-
ja upande wake wa kuume na
mwingine upande wake wa ku-
shoto.[a] **28** —— **29** Na wale
waliokuwa wakipitia hapo wa-
likuwa wakimtukana,[b] waki-
tikisa vichwa vyao na kuse-
ma: "Po! Wewe uliyetaka ku-
liangusha hekalu na kulije-
nga kwa siku tatu,[c] **30** jiokoe
mwenyewe kwa kushuka ku-
toka kwenye mti wa mate-
so."[d] **31** Vivyo hivyo pia wa-
kuu wa makuhani walikuwa
wakimdhihaki katikati yao we-
nyewe pamoja na waandishi
na kusema: "Aliwaokoa wengi-
ne; hawezi kujiokoa mwenye-
we![e] **32** Acheni Kristo Mfa-
lme wa Israeli ashuke sasa ku-
toka kwenye mti wa mateso,
ili tupate kuona na kuamini."[f]
Hata wale waliotundikwa mti-
ni pamoja naye walikuwa waki-
mshutumu.[g]
33 Ilipofika saa sita kuka-
wa na giza juu ya nchi yote
mpaka saa tisa.[h] **34** Na saa
tisa Yesu akapaaza kilio kwa
sauti kubwa: *"Eli, Eli, lama
sabakthani?"* maneno ambayo
yanapotafsiriwa humaanisha:
"Mungu wangu, Mungu wa-
ngu, kwa nini umeniacha?"[i]
35 Na baadhi ya wale wali-
okuwa wamesimama karibu,
waliposikia, wakaanza kuse-
ma: "Tazama! Anamwita Eli-
ya."[j] **36** Lakini mtu fulani
akakimbia, akalowesha sifo-
ngo katika divai kali, akaiwe-
ka juu ya utete, na kuanza ku-
mnywesha,[k] akisema: "Acheni
iwe hivyo kwake! Acheni tuone
kama Eliya atakuja kumshu-
sha."[l] **37** Lakini Yesu akatoa
kilio kikubwa, akakata pumzi.[m]
38 Na pazia[n] la patakatifu li-

SURA 15
a Mt 27:26
Yoh 19:1
b Mt 27:27
c Mt 27:28
d Mt 27:29
Yoh 19:3
e Mt 27:30
f Mt 27:31
Yoh 19:16
g Mt 27:32
Lu 23:26
h Mt 27:33
Lu 23:33
Yoh 19:17
Ebr 13:12
i Zb 69:21
j Mt 27:34
k Zb 22:18
l Mt 27:35
Yoh 19:23
m Mt 27:45
Lu 23:44
Yoh 19:14
n Mt 27:29
o Mt 27:37
Lu 23:38
Yoh 19:19

Safu ya 2
a Mt 27:38
b Zb 22:7
Zb 109:25
Isa 53:3
c Mt 27:40
Mk 14:58
d Lu 23:35
e Mt 27:41
f Mt 16:4
Mt 27:42
Ro 3:3
g Mt 27:44
1Pe 2:23
h Mt 27:45
Lu 23:44
i Zb 22:1
Mt 27:46
j Mt 27:47
k Zb 69:21
Mt 27:48
Yoh 19:29
l Mt 27:49
m Zb 31:5
Mt 27:50
Lu 23:46
Yoh 19:30
n Kut 26:31
Ebr 6:19
Ebr 10:20

kapasuka vipande viwili kutoka juu mpaka chini.[a] **39** Sasa yule ofisa-jeshi aliyekuwa amesimama kando yake akimtazama, alipoona kwamba amekufa katika hali hizo, akasema: "Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu."[b]

40 Kulikuwa pia na wanawake wakitazama wakiwa mbali,[c] kati yao Maria Magdalene na vilevile Maria mama ya Yakobo Mdogo na Yose, na Salome,[d] **41** waliokuwa na kawaida ya kufuatana naye[e] na kumhudumia alipokuwa Galilaya, na wanawake wengine wengi waliokuwa wamekuja na kupanda pamoja naye mpaka Yerusalemu.[f]

42 Sasa kwa kuwa ilikuwa jioni, na kwa kuwa yalikuwa ni Matayarisho, yaani, siku inayotangulia sabato, **43** Yosefu wa Arimathea, mshiriki wa Baraza mwenye kusifika, ambaye pia alikuwa akiungojea ufalme wa Mungu, akaja.[g] Akajipa moyo kuingia mbele ya Pilato na kuomba apewe mwili[h] wa Yesu. **44** Lakini Pilato akataka kujua kama tayari alikuwa amekufa, akamwita yule ofisa-jeshi, akamuuliza kama tayari alikuwa amekufa. **45** Kwa hiyo baada ya kuhakikisha kutoka kwa huyo ofisa-jeshi, akampa Yosefu maiti hiyo.[i] **46** Basi akanunua kitani bora na kumshusha, akamfunga katika kile kitani bora na kumlaza[j] katika kaburi[k] lililokuwa limechimbwa katika mwamba; naye akaviringisha jiwe hata kwenye mlango wa lile kaburi.[l] **47** Lakini Maria Magdalene na Maria mama ya Yose wakaendelea kutazama mahali alipokuwa amelazwa.[a]

16 Kwa hiyo siku ya sabato[b] ilipokuwa imepita, Maria Magdalene,[c] na Maria mama ya Yakobo, na Salome wakanunua manukato kusudi waje kumpaka.[d] **2** Na mapema sana siku ya kwanza[e] ya juma wakaja kwenye kaburi, jua lilipokuwa limechomoza.[f] **3** Nao walikuwa wakisemezana: "Ni nani atakayetuviringishia lile jiwe kutoka kwenye mlango wa kaburi?" **4** Lakini walipotazama juu, wakaona kwamba jiwe lilikuwa limeviringishwa, ijapokuwa lilikuwa kubwa sana.[g] **5** Walipoingia ndani ya kaburi, wakaona kijana ameketi upande wa kuume akiwa amevaa kanzu nyeupe, nao wakafadhaika.[h] **6** Akawaambia: "Acheni kufadhaika. Mnamtafuta Yesu Mnazareti, aliyetundikwa mtini.[i] Alifufuliwa,[j] hayupo hapa. Tazameni! Mahali walipomlaza.[k] **7** Lakini nendeni, mkawaambie wanafunzi wake na Petro, 'Yeye anawatangulia kuingia Galilaya;[l] huko mtamwona, kama vile alivyowaambia ninyi.'"[m] **8** Kwa hiyo walipotoka wakakimbia kutoka kwenye kaburi, kwa maana walikuwa wakitetemeka nao walikuwa na hisia nyingi. Nao hawakumwambia mtu jambo lolote, kwa maana walikuwa wanaogopa.[n]

SURA 15

a Mt 27:51 Lu 23:45
b Mt 27:54 Lu 23:47
c Zb 38:11
d Mt 27:56
e Lu 8:2
f Lu 23:49
g Mt 27:57 Yoh 19:38
h Kum 21:23
i Mt 27:58
j Isa 53:9 Mt 27:59
k Mdo 13:29
l Mt 27:60 Lu 23:53 Yoh 19:40

Safu ya 2

a Mt 27:61 Lu 23:55

SURA 16

b Kut 20:8
c Mt 28:1
d Mk 14:8 Lu 23:56
e Lu 24:1
f Yoh 20:1
g Lu 24:2
h Lu 24:3 Yoh 20:11
i Mt 28:5 Lu 24:4
j Mk 8:31 Lu 18:33 Mdo 4:10
k Mt 28:6
l Mt 26:32 Mt 28:7
m Mk 14:28
n Mt 28:8 Lu 24:9

UMALIZIO MREFU

Hati nyingine za kale (Codex Alexandrinus, Codex Ephraemi, Codex Bezae) na tafsiri (Latin *Vulgate,* Curetonian Syriac, Syriac *Peshitta*) huongeza umalizio mrefu unaofuata, lakini ambao Codex Sinaiticus, Codex

Vaticanus, Sinaitic Syriac codex, na Armenian Version huondoa:

9 Baada ya kufufuka mapema siku ya kwanza ya juma akamtokea kwanza Maria Magdalene, ambaye alikuwa amefukuza roho waovu saba kutoka kwake. **10** Maria Magdalene akaenda, akawaambia wale waliokuwa wamekuwa pamoja na Yesu, kwa maana walikuwa wakiomboleza na kulia. **11** Lakini wao, waliposikia alikuwa amefufuka na Maria Magdalene alikuwa amemwona, hawakuamini. **12** Tena, baada ya mambo hayo aliwatokea katika umbo lingine wawili kati yao wakitembea, walipokuwa wakienda mashambani; **13** nao wakarudi wakawaambia wale wengine. Wala hawakuwaamini. **14** Lakini baadaye akawatokea wale kumi na mmoja wenyewe walipokuwa wameketi mezani, naye akaushutumu ukosefu wao wa imani na ugumu wa moyo, kwa sababu hawakuwaamini wale waliokuwa wamemwona sasa akiwa amefufuka kutoka kwa wafu. **15** Naye akawaambia: "Nendeni, mkaingie katika ulimwengu wote na kuhubiri habari njema kwa uumbaji wote. **16** Yeye anayeamini na kubatizwa ataokolewa, lakini yule ambaye hataamini atahukumiwa adhabu. **17** Zaidi ya hayo, ishara hizi zitafuatana na wale wanaoamini: Kwa kutumia jina langu watatoa roho waovu, watasema kwa lugha, **18** nao watainua nyoka kwa mikono yao, na wakinywa kitu chochote chenye kuua hakitawaumiza hata kidogo. Wataweka mikono yao juu ya watu wagonjwa, nao watapona."

19 Kwa hiyo, basi, Bwana Yesu, alipokuwa amekwisha kusema nao, akachukuliwa juu mpaka mbinguni na kuketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu. **20** Basi, wakatoka kwenda na kuhubiri kila mahali, huku Bwana akifanya kazi pamoja nao na kuutegemeza ujumbe huo kupitia ishara zenye kufuatana nao.

UMALIZIO MFUPI

Hati na tafsiri fulani za mwishomwisho zina umalizio mfupi baada ya Marko 16:8, kama ifuatavyo:

Lakini mambo yote yaliyokuwa yameamriwa wakayasimulia kwa ufupi kwa wale waliomzunguka Petro. Tena, baada ya mambo hayo, Yesu mwenyewe akapeleka kupitia wao tangazo takatifu na lisiloweza kuharibika la wokovu wa milele kutoka mashariki mpaka magharibi.

KULINGANA NA

LUKA

1 Kwa kuwa wengi wamechukua daraka la kukusanya habari za mambo ya hakika[a] tunayosadiki kikamili kati yetu, **2** sawa na vile wale ambao tangu mwanzo[b] walikuwa mashahidi wa kujionea[c] na watumishi wa ujumbe[d] walivyotuletea haya, **3** mimi pia niliazimia, kwa sababu nimefuata kwa uangalifu mambo yote tangu mwanzo kwa usahihi, kukuandikia hayo kwa utaratibu wenye kufuatana,[e] mtukufu[f] Theofilo,[g] **4** ili upate kujua kabisa uhakika wa mambo ambayo umefundishwa kwa mdomo.[a]

5 Katika siku za Herode,[b] mfalme wa Yudea, kulikuwa na kuhani aliyeitwa Zekaria wa mgawanyo wa Abiya,[c] naye alikuwa na mke kutoka kwa binti za Haruni,[d] na jina lake lilikuwa Elisabeti. **6** Wote wawili walikuwa waadilifu[e] mbele za Mungu kwa sababu ya kutembea bila lawama[f] kulingana na amri[g] zote na matakwa ya kisheria[h] ya Yehova.[i] **7** Laki-

SURA 1

a Yoh 20:31
b Mk 1:1
1Yo 1:1
c Yoh 15:27
1Pe 5:1
2Pe 1:16
d Mdo 6:4
Ebr 2:3
e 1Ko 14:40
f Mdo 24:3
g Mdo 1:1

Safu ya 2

a Yoh 20:31
Mdo 18:25
Ga 6:6
b Mt 2:1
c 1Nya 24:10
d Law 21:14
e Mwa 7:1
Flp 3:6
f Ayu 1:1
g 1Fa 9:4
2Fa 20:3
Zb 119:6
h Ebr 9:10

i Law 18:5; Law 20:8; Zb 119:1.

ni hawakuwa na mtoto, kwa
sababu Elisabeti alikuwa tasa,[a]
nao wote wawili walikuwa wa-
mesonga sana katika miaka.

8 Basi alipokuwa akitenda
akiwa kuhani katika mgawo
wa mgawanyo[b] wake mbele za
Mungu, **9** kulingana na de-
sturi ya cheo cha kikuhani
ikawa zamu yake kutoa uvu-
mba[c] alipoingia katika pataka-
tifu pa Yehova;[d] **10** na uma-
ti wote wa watu ulikuwa uki-
sali nje katika saa hiyo ya
kutoa uvumba.[e] **11** Malaika
wa Yehova akamtokea, akiwa
amesimama upande wa kuu-
me wa madhabahu ya uvumba.[f]
12 Lakini Zekaria akataabi-
shwa na jambo hilo aliloona, na
woga ukamwingia.[g] **13** Hata
hivyo, malaika akamwambia:
"Usiogope, Zekaria, kwa saba-
bu dua yako imekubaliwa,[h] na
mke wako Elisabeti atamzaa
mwana wako, nawe utamwi-
ta jina lake Yohana.[i] **14** Nawe
utakuwa na shangwe na fu-
raha kubwa, na wengi wata-
shangilia[j] kuzaliwa kwake;
15 kwa maana atakuwa mkuu
mbele za Yehova.[k] Lakini asi-
nywe divai na kileo hata kido-
go,[l] naye atajazwa roho takati-
fu akiwa katika tumbo la uza-
zi la mama yake;[m] **16** naye
atawarudisha wengi wa wana
wa Israeli kwa Yehova[n] Mungu
wao. **17** Pia, atakwenda mbe-
le zake kwa roho na nguvu za
Eliya,[o] ili kurudisha mioyo[p] ya
akina baba kwa watoto na wale
wasiotii kwenye hekima inayo-
tumika ya waadilifu, ili kuwe-
ka tayari kwa ajili ya Yehova[q]
watu waliotayarishwa."[r]

18 Naye Zekaria akamwa-
mbia malaika: "Nitakuwaje na
uhakika juu ya jambo hili?
Kwa maana nina umri mku-
bwa[a] na mke wangu amesonga
sana katika miaka." **19** Mala-
ika akamjibu akamwambia:
"Mimi ni Gabrieli,[b] anayesima-
ma karibu mbele za Mungu,
nami nilitumwa kusema[c] na
wewe na kukutangazia ha-
bari njema ya mambo hayo.
20 Lakini, tazama! utakuwa
kimya[d] nawe hutaweza kuse-
ma mpaka siku ambayo ma-
mbo hayo yatatendeka, kwa
sababu hukuamini maneno ya-
ngu, ambayo yatatimizwa kati-
ka wakati wake uliowekwa."
21 Wakati huohuo watu wa-
kaendelea kumngoja Zekaria,[e]
nao wakaanza kustaajabia ku-
kawia kwake katika pataka-
tifu. **22** Lakini alipotoka ha-
kuweza kusema nao, nao waka-
fahamu kwamba alikuwa ame-
ona maono yanayozidi nguvu
za asili[f] ndani ya patakatifu;
naye akawa anawatolea ishara,
lakini akaendelea kuwa bubu.
23 Basi, siku za utumishi wake
wa watu wote zilipotimia,[g] aka-
enda nyumbani kwake.

24 Lakini baada ya siku
hizo Elisabeti mke wake aka-
pata mimba;[h] naye akajitenga
kwa miezi mitano, akisema:
25 "Hivi ndivyo Yehova ame-
shughulika nami siku hizi wa-
kati amenipa uangalifu wake
ili kuondolea mbali shutuma
yangu katikati ya watu."[i]

26 Katika mwezi wake wa
sita malaika Gabrieli[j] alitu-
mwa kutoka kwa Mungu mpa-
ka jiji moja la Galilaya linaloi-
twa Nazareti, **27** kwa bikir-
a aliyechumbiwa na mwana-
mume anayeitwa Yosefu wa

SURA 1

a Mwa 18:11
b 1Nya 24:19
2Nya 8:14
2Nya 31:2
c Kut 30:7
d Kut 40:5
e Ufu 8:3
f Mdo 10:3
g Amu 6:22
Da 10:8
Mdo 10:4
Ufu 1:17
h Da 10:12
i Mwa 17:19
Lu 1:60
j Lu 1:58
k Lu 7:28
l Hes 6:3
Amu 13:4
Mt 11:18
m Yer 1:5
Ro 9:11
Ga 1:15
n Mal 4:6
o Mt 11:14
Mt 17:10
p Mal 4:6
q Isa 40:3
r 1Sa 7:3
Mal 3:1

Safu ya 2

a Mwa 17:17
Mwa 18:11
Ro 4:19
b Da 8:16
Da 9:21
Ebr 1:14
c Lu 1:26
d Eze 3:26
Eze 24:27
e Hes 6:23
f 2Ko 12:1
g 1Nya 9:25
h Mt 1:18
i Mwa 30:23
1Sa 1:11
j Da 8:16
Lu 1:19

nyumba ya Daudi; na jina la
bikira[a] huyo lilikuwa Maria.[b]
28 Na Gabrieli alipoingia mbe-
le yake akasema: "Siku nje-
ma,[c] uliyependelewa sana, Ye-
hova[d] yuko pamoja nawe."[e]
29 Lakini Maria akashtushwa
sana na maneno hayo na
kuanza kuwaza hiyo ingewe-
za kuwa ni salamu ya namna
gani. **30** Kwa hiyo malaika
akamwambia: "Usiogope, Ma-
ria, kwa maana umepata ki-
bali[f] cha Mungu; **31** na, ta-
zama! utachukua mimba kati-
ka tumbo lako la uzazi na ku-
zaa mwana,[g] nawe utamwita
jina lake Yesu.[h] **32** Huyo ata-
kuwa mkuu[i] naye ataitwa Mwa-
na wa Aliye Juu Zaidi;[j] na Ye-
hova Mungu atampa kiti cha
ufalme[k] cha Daudi baba yake,[l]
33 naye atatawala akiwa mfa-
lme juu ya nyumba ya Yakobo
milele, na ufalme wake hauta-
kuwa na mwisho."[m]

34 Lakini Maria akamwa-
mbia malaika: "Hilo litawezе-
kanaje, kwa kuwa silali[n] na
mwanamume?" **35** Malaika
akamjibu akamwambia: "Roho
takatifu[o] itakuja juu yako, na
nguvu za Aliye Juu Zaidi zi-
takufunika. Kwa sababu hiyo
pia kile kitakachozaliwa kitai-
twa kitakatifu,[p] Mwana wa Mu-
ngu.[q] **36** Na, tazama! Elisabe-
ti mtu wa jamaa yako, yeye pia
amechukua mimba ya mwana,
katika uzee wake, na huu ni
mwezi wake wa sita, yeye amba-
ye huitwa mwanamke tasa;[r]
37 kwa sababu kwa Mungu ha-
kuna tangazo lolote lisilowezе-
kana."[s] **38** Ndipo Maria aka-
sema: "Tazama! Kijakazi[t] wa
Yehova! Na itendeke kwangu
kulingana na tangazo lako."
Ndipo malaika akaondoka.

39 Basi Maria akaondoka
katika siku hizo akaenda ha-
raka katika nchi yenye mili-
ma, mpaka jiji moja la Yuda,
40 naye akaingia nyumbani
mwa Zekaria akamsalimu Elisa-
beti. **41** Basi, Elisabeti ali-
posikia salamu za Maria, yule
mtoto mchanga katika tumbo
lake la uzazi akaruka; na Elisa-
beti akajazwa roho taka-
tifu, **42** naye akapaaza sau-
ti kubwa na kusema: "Wewe ni
mbarikiwa kati ya wanawake,
na uzao wa tumbo lako la uzazi
umebarikiwa![a] **43** Basi ime-
wezekanaje nikapata pendeleo
hili, kwamba mama ya Bwana[b]
wangu aje kwangu? **44** Kwa
maana, tazama! Niliposikia sa-
lamu zako, mtoto katika tu-
mbo langu la uzazi aliruka kwa
furaha kubwa.[c] **45** Mwenye
furaha pia ni yule aliyeami-
ni, kwa sababu kutakuwa uti-
mizo kamili[d] wa mambo aliyoa-
mbiwa kutoka kwa Yehova."[e]

46 Naye Maria akasema:
"Nafsi yangu inamtukuza Ye-
hova,[f] **47** na roho yangu hai-
wezi kuacha kumfurahia[g] Mu-
ngu Mwokozi[h] wangu; **48** kwa
sababu ametazama hali ya chi-
ni ya kijakazi[i] wake. Kwa maa-
na, tazama! tangu sasa na ku-
endelea vizazi vyote vitanita-
ngaza kuwa mwenye furaha;[j]
49 kwa sababu Mwenye nguvu
amenitendea makuu, nalo jina
lake ni takatifu;[k] **50** na kwa
vizazi baada ya vizazi rehe-
ma yake iko juu ya wale wa-
naomwogopa.[l] **51** Ametenda
kwa nguvu kwa mkono wake,[m]
amewatawanya kotekote wale

SURA 1

a Isa 7:14
b Mt 1:18
Lu 2:5
c Mt 26:49
Mk 15:18
Yoh 19:3
d Yer 1:19
e Amu 5:24
f Met 12:2
g Mwa 16:11
Amu 13:3
Ga 4:4
h Mt 1:21
Lu 2:21
i Flp 2:10
1Ti 6:15
j Mt 27:54
Yoh 1:49
k 2Sa 7:12
Zb 132:11
Isa 9:7
Yer 23:5
l Isa 11:1
Isa 11:10
Mt 1:1
m Da 2:44
Da 7:14
Ebr 1:8
n Isa 7:14
Mt 1:25
o Mt 1:18
Mt 1:20
p Yoh 6:69
Yoh 10:36
q Mt 14:33
Yoh 1:34
Yoh 20:31
Ro 1:4
r Mwa 11:30
Zb 113:9
s Mwa 18:14
Zb 115:3
Yer 32:17
Zek 8:6
Mt 19:26
t 1Sa 1:11

Safu ya 2

a Kum 28:4
Lu 11:27
b Mt 3:11
c Yoh 3:29
d Ebr 11:11
e Mwa 18:14
Mwa 21:1
f 1Sa 2:1
Zb 34:2
g Hab 3:18
h 2Sa 22:3
Isa 43:3
Tit 1:3
Yud 25
i 1Sa 1:11
Zb 138:6
j Lu 11:27
k Zb 71:19
Zb 111:9
Isa 57:15
l Kut 20:6
Zb 103:17
m Zb 89:10
Isa 40:10
Isa 52:10

wenye majivuno katika kusudi
la mioyo yao.[a] **52** Amewashu-
sha watu wenye nguvu[b] kuto-
ka katika viti vya ufalme na ku-
wainua watu wa hali ya chini;[c]
53 amewashibisha kabisa we-
nye njaa kwa vitu vyema[d] na
wale waliokuwa na mali ame-
waacha waende mikono mitu-
pu.[e] **54** Amekuja kumsaidia
Israeli mtumishi wake,[f] kuku-
mbuka rehema,[g] **55** sawa na
vile alivyowaambia mababu
zetu, Abrahamu na uzao wake,
milele."[h] **56** Maria akakaa
pamoja naye kwa karibu mi-
ezi mitatu, akarudi nyumbani
kwake.

57 Sasa wakati ukafika wa
Elisabeti kuzaa, naye akazaa
mwana. **58** Nao majirani na
watu wa jamaa yake wakasi-
kia kwamba Yehova alikuwa
ameitukuza rehema[i] yake kwa-
ke, nao wakaanza kushangi-
lia[j] pamoja naye. **59** Na ka-
tika siku ya nane wakaja ku-
mtahiri huyo mtoto mchanga,[k]
nao walitaka kumwita kwa
jina la baba yake, Zekaria.
60 Lakini mama yake akajibu
akasema: "Sivyo hata kidogo!
bali ataitwa Yohana." **61** Ndi-
po wakamwambia: "Hakuna
yeyote kati ya watu wa jamaa
yako anayeitwa kwa jina hilo."
62 Ndipo wakaanza kumuu-
liza baba yake kwa ishara
jina ambalo alitaka aitwe.
63 Naye akaomba bamba na
kuandika: "Yohana[l] ndilo jina
lake." Ndipo wote wakastaaja-
bu. **64** Kinywa chake kikafu-
nguka[m] mara moja na ulimi
wake ukalegea naye akaanza
kuongea, akimbariki Mungu.
65 Na wale wote waliokuwa
wakiishi katika ujirani wao
wakaingiwa na woga; na kati-
ka nchi yote ya milima ya Yu-
dea mambo yote hayo yakaa-
nza kuzungumzwa pande zote,
66 na wote waliosikia wakali-
weka mioyoni[a] mwao, wakise-
ma: "Kwa kweli mtoto huyu
mchanga atakuwa wa namna
gani?" Kwa maana kwa kweli
mkono[b] wa Yehova ulikuwa pa-
moja naye.

67 Na Zekaria baba yake aka-
jazwa roho takatifu,[c] naye akatoa
unabii,[d] akisema: **68** "Na abari-
kiwe Yehova Mungu wa Israeli,[e]
kwa sababu ameelekeza uanga-
lifu wake na kufanya ukombozi[f]
kuelekea watu wake.[g] **69** Naye
ametuinulia pembe[h] ya wokovu
katika nyumba ya Daudi mtu-
mishi wake, **70** sawa na vile,
kupitia kinywa cha manabii
wake watakatifu tangu zama-
ni za kale,[i] amesema **71** juu
ya wokovu kutoka kwa adui
zetu na kutoka katika mko-
no wa wale wote wanaotuchu-
kia;[j] **72** kufanya rehema ku-
husiana na mababu zetu na
kulikumbuka agano lake taka-
tifu,[k] **73** kiapo ambacho ali-
mwapia Abrahamu babu yetu,[l]
74 kutupa sisi, baada ya ku-
kolewa kutoka katika miko-
no ya adui,[m] pendeleo la ku-
mtolea utumishi mtakatifu bila
woga[n] **75** kwa ushikamani-
fu na uadilifu mbele zake
siku zetu zote.[o] **76** Na wewe,
mtoto mchanga, utaitwa nabii
wa Aliye Juu Zaidi, kwa maa-
na utakwenda mbele za Yeho-
va ili kutayarisha njia zake,[p]
77 kuwapa watu wake ujuzi
wa wokovu kwa msamaha wa
dhambi zao,[q] **78** kwa sababu
ya huruma nyororo za Mungu

SURA 1

a 2Sa 22:28
Da 4:37
1Pe 5:5
b Ayu 12:19
Isa 22:19
Isa 40:23
c 1Sa 2:6
d 1Sa 2:5
Zb 34:10
Zb 107:9
e Isa 65:13
f Isa 44:21
g Zb 98:3
Isa 41:8
Yer 31:3
h Mwa 17:19
Mik 7:20
Ga 3:16
i Zb 113:9
Zb 116:5
j Lu 1:14
Ro 12:15
k Mwa 17:12
Law 12:3
Flp 3:5
l Lu 1:13
m Lu 1:20

Safu ya 2

a Lu 2:19
b Mwa 39:2
Zb 80:17
c Hes 11:25
2Sa 23:2
d 2Pe 1:21
e 1Fa 1:48
Zb 41:13
Zb 72:18
Zb 106:48
f Zb 111:9
Lu 7:16
g Kum 7:6
Zb 135:4
h 1Sa 2:10
Zb 132:17
i Yer 23:5
Da 9:24
j Zb 106:10
k Mwa 17:7
Law 26:42
Kum 4:31
Kum 7:12
Zb 105:8
Zb 106:45
l Mwa 22:16
Mik 7:20
Ebr 6:13
m Yer 30:8
Ro 6:22
n Yer 30:9
Ebr 9:14
o Ga 4:4
p Isa 40:3
Mal 3:1
Mt 3:3
q Mk 1:4

wetu. Kwa huruma hizo tutapata pambazuko[a] kutoka juu,[b]
79 kuwapa nuru wale wanaokaa katika giza na katika kivuli[c] cha kifo, kuelekeza kwa mafanikio miguu yetu katika njia ya amani."

80 Na huyo mtoto mchanga akaendelea kukua[d] na kupata nguvu katika roho, naye akakaa katika majangwa mpaka siku ya kujionyesha waziwazi kwa Israeli.

2 Basi katika siku hizo Kaisari Augusto alitoa amri[e] kwamba dunia yote inayokaliwa iandikishwe; **2** (uandikisho huu wa kwanza ulitendeka wakati Kirenio alipokuwa gavana wa Siria;) **3** na watu wote wakaanza kusafiri kwenda kuandikishwa,[f] kila mmoja kwenye jiji lake mwenyewe. **4** Yosefu pia akapanda kutoka Galilaya, kutoka jiji la Nazareti, akaingia Yudea, kwenye jiji la Daudi, linaloitwa Bethlehemu,[g] kwa sababu alikuwa mshiriki wa nyumba na familia ya Daudi,[h] **5** ili apate kuandikishwa pamoja na Maria,[i] aliyekuwa amemwoa kama ilivyoahidiwa,[j] wakati huu akiwa karibu kuzaa.[k] **6** Walipokuwa huko, siku zikatimia apate kuzaa. **7** Naye akamzaa mwana wake, mzaliwa wa kwanza,[l] akamfunga vitambaa na kumlaza katika hori,[m] kwa sababu hapakuwa na mahali kwa ajili yao katika chumba cha kukaa.

8 Katika nchi hiyo kulikuwako pia wachungaji wakiishi nje, wakichunga makundi yao usiku. **9** Na kwa ghafula malaika[n] wa Yehova akasimama kando yao, na utukufu[a] wa Yehova ukamulika pande zote kuwazunguka, nao wakaogopa sana. **10** Lakini malaika akawaambia: "Msiogope, kwa maana, tazama! ninawatangazia ninyi habari njema ya shangwe kubwa ambayo watu wote watakuwa nayo,[b]
11 kwa sababu leo katika jiji la Daudi,[c] Mwokozi[d] ambaye ni Kristo Bwana,[e] amezaliwa kwenu.[f] **12** Na hii ndiyo ishara kwenu: Mtamkuta mtoto akiwa amefungwa vitambaa na akiwa amelala katika hori."
13 Na kwa ghafula umati wa jeshi la mbingu[g] ukawa pamoja na yule malaika, ukimsifu Mungu[h] na kusema: **14** "Utukufu katika vilele vilivyo juu[i] kwa Mungu, na juu ya dunia amani[j] kati ya watu wa nia njema."[k]

15 Kwa hiyo malaika walipokuwa wameondoka na kuingia mbinguni, wachungaji wakaanza kusemezana: "Na twende moja kwa moja mpaka Bethlehemu tukaone jambo hili ambalo limetendeka, ambalo Yehova[l] ametujulisha." **16** Nao wakaenda haraka wakamkuta Maria na vilevile Yosefu, na yule mtoto mchanga akiwa amelala katika hori. **17** Walipomwona, wakasema mambo yaliyokuwa yamesemwa kuhusu mtoto huyo mchanga. **18** Na wote waliosikia wakastaajabu juu ya mambo waliyoambiwa na wachungaji, **19** lakini Maria akaanza kuyahifadhi maneno hayo yote, akikata kauli moyoni mwake.[m] **20** Basi wachungaji wakarudi, wakimtukuza na kumsifu Mungu kwa ajili ya

SURA 1
a Zb 97:11
b Isa 11:1
c Zb 107:10
Isa 9:2
Isa 49:9
Isa 59:9
Mt 4:16
Mdo 26:18
d Lu 2:40

SURA 2
e Da 11:20
f Ro 13:1
g 1Sa 16:1
Mik 5:2
Mt 2:6
h Mt 1:16
i Lu 1:27
j Mt 1:25
Lu 1:27
k Mt 1:18
l Mt 1:25
m Isa 53:2
n Ebr 1:14

Safu ya 2
a Law 9:6
b Mwa 12:3
Mdo 13:48
c 1Sa 20:6
d Isa 19:20
e Mdo 2:36
Flp 2:11
f Isa 9:6
g Zb 103:21
h Mwa 28:12
Da 7:10
Ebr 1:14
Ufu 5:11
i Zb 148:1
Mk 11:10
j Isa 57:19
Kol 1:20
k Zb 30:5
Isa 61:2
Lu 19:38
l Zb 111:2
m Mwa 37:11
Lu 1:66
Lu 2:51

mambo yote waliyoyasikia na
kuyaona, sawa na walivyoku-
wa wameambiwa.
21 Basi siku nane[a] zilipoti-
mia ili kumtahiri,[b] akaitwa pia
jina lake Yesu,[c] lile jina aliloi-
twa na malaika kabla hajachu-
kuliwa mimba katika tumbo la
uzazi.[d]
22 Pia, siku za kuwataka-
sa[e] hao kulingana na sheria ya
Musa zilipotimia, wakamleta
Yesu mpaka Yerusalemu ili ku-
mtoa kwa Yehova, **23** sawa
na vile ambavyo imeandi-
kwa katika sheria ya Yehova:
"Kila mtoto wa kiume anaye-
fungua tumbo la uzazi lazima
aitwe mtakatifu kwa Yehova,"[f]
24 na kutoa dhabihu kulinga-
na na yanayosemwa katika
sheria ya Yehova: "Njiwa-te-
tere wawili au hua wachanga
wawili."[g]
25 Na, tazama! palikuwa na
mtu mmoja katika Yerusale-
mu aliyeitwa Simeoni, na
mtu huyo alikuwa mwadilifu
na mwenye kumheshimu Mu-
ngu, akingojea faraja ya Israe-
li,[h] na roho takatifu ilikuwa juu
yake. **26** Zaidi ya hayo, ali-
kuwa amefunuliwa kimungu na
roho takatifu kwamba hangeo-
na kifo kabla ya kumwona Kri-
sto[i] wa Yehova. **27** Akaja sasa
katika hekalu chini ya ngu-
vu za roho;[j] na wazazi walipo-
mwingiza mtoto mchanga Yesu
ili kufanya kwa ajili yake ku-
lingana na zoea la kidesturi la
sheria,[k] **28** Simeoni mwenye-
we akampokea mtoto mikononi
mwake akambariki Mungu na
kusema: **29** "Sasa, Bwana
Mwenye Enzi Kuu, unamwa-
cha mtumwa wako aende aki-
wa huru[a] kwa amani kulingana
na tangazo lako; **30** kwa saba-
bu macho yangu yameona njia
yako ya kuokoa[b] **31** ambayo
umetayarisha mbele ya viku-
ndi vyote vya watu,[c] **32** nuru[d]
ya kuondoa utaji[e] kwa mataifa[f]
na utukufu wa watu wako
Israeli." **33** Na baba na mama
yake wakaendelea kustaajabia
mambo yaliyokuwa yakisemwa juu yake. **34** Pia, Simeoni akawabariki wao, lakini akamwambia Maria mama yake: "Tazama! Huyu amewekwa kwa ajili ya kuanguka[g] na kusimama tena kwa wengi katika Israeli[h] na kuwa ishara itakayosemwa vibaya[i] **35** (ndiyo, upanga mrefu utaichoma nafsi yako),[j] ili mawazo ya mioyo mingi yapate kufunuliwa."[k]
36 Basi kulikuwako nabii Ana, binti ya Fanueli, wa kabila la Asheri (mwanamke huyu alikuwa amesonga sana katika miaka, na alikuwa ameishi pamoja na mume kwa miaka saba kutoka ubikira wake, **37** naye sasa alikuwa mjane[l] mwenye umri wa miaka 84), ambaye alikuwa hakosi kamwe kuwa katika hekalu, akitoa utumishi mtakatifu usiku na mchana[m] kwa kufunga na dua. **38** Na saa ileile akakaribia, akaanza kumshukuru Mungu akisema juu ya mtoto huyo kwa wale wote waliokuwa wakiungojea ukombozi wa Yerusalemu.[n]
39 Kwa hiyo walipokuwa wametimiza mambo yote kulingana na sheria[o] ya Yehova, wakarudi kuingia Galilaya kwenye jiji la kwao la Nazareti.[p] **40** Na huyo mtoto

SURA 2
a Mwa 17:12
Law 12:3
Ga 4:4
b Mwa 17:10
c Mt 1:21
d Lu 1:31
e Law 12:2
f Kut 13:2
Kut 22:29
Kut 34:19
Hes 3:13
Hes 8:17
g Law 1:14
Law 5:7
Law 12:8
h Zb 119:166
Isa 40:1
Isa 49:13
i Lu 9:20
j Mdo 8:29
k Law 12:6

Safu ya 2
a Mwa 46:30
Isa 57:2
b Isa 52:10
Lu 3:6
Mdo 4:12
c Isa 40:5
Isa 42:1
d Isa 9:2
Isa 60:1
Mt 4:16
e Isa 25:7
f Isa 11:10
Isa 42:6
Isa 49:6
Mdo 13:47
Mdo 26:23
g Isa 53:10
h Isa 8:14
Ho 14:9
1Ko 1:23
1Pe 2:8
i Mdo 28:22
1Pe 2:12
j Yoh 19:25
k 1Ko 11:19
l 1Ti 5:5
m Mdo 26:7
n Isa 52:9
Omb 3:26
Mk 15:43
Lu 2:25
o Law 12:6
p Mt 2:23
Lu 1:26

mchanga akaendelea kukua
na kupata nguvu,[a] akijawa na
hekima, na kuendelea kuwa na
kibali[b] cha Mungu.
41 Basi wazazi wake wali-
kuwa na desturi ya kwenda
Yerusalemu[c] mwaka baada ya
mwaka kwa ajili ya sherehe
ya pasaka. **42** Na alipofika
umri wa miaka kumi na miwi-
li, walipanda kulingana na de-
sturi[d] ya sherehe **43** waka-
zikamilisha siku. Lakini wali-
pokuwa wakirudi, mvulana
huyo, Yesu, alibaki nyuma Ye-
rusalemu, na wazazi wake ha-
wakutambua. **44** Wakidha-
ni kwamba alikuwa katika-
ti ya kundi lililokuwa likisafi-
ri pamoja, walisafiri umbali[e]
wa siku moja, kisha wakaanza
kumtafuta kwa bidii kati ya
jamaa zao na wale wanaojua-
na nao. **45** Lakini, walipoko-
sa kumpata, wakarudi mpaka
Yerusalemu, wakimtafuta kwa
bidii. **46** Basi, baada ya siku
tatu wakampata katika heka-
lu,[f] ameketi katikati ya wali-
mu, akiwasikiliza na kuwau-
liza maswali. **47** Lakini wale
wote waliokuwa wakimsikiliza
walikuwa wakishangazwa daima
na uelewaji wake na majibu
yake.[g] **48** Basi walipomwo-
na wakastaajabu, na mama
yake akamwambia: "Mtoto,
kwa nini umetutendea hivi?
Tazama, baba yako nami tume-
kuwa tukikutafuta tukiwa na
hangaiko la akilini." **49** La-
kini akawaambia: "Kwa nini
mlilazimika kunitafuta? Je,
hamkujua kwamba ni lazima
niwe katika nyumba ya Baba
yangu?"[h] **50** Hata hivyo, ha-
wakufahamu maneno hayo ali-
yowaambia.[i]

SURA 2
a Lu 1:80
Lu 2:52
b Isa 11:2
c Kut 23:14
Kum 16:16
d Kut 34:23
e 1Fa 19:4
f Mt 26:55
g Zb 119:99
Mt 7:28
Mk 1:22
Yoh 7:15
h Zb 26:8
Zb 27:4
Met 20:11
Yoh 2:16
i Lu 9:45
Lu 18:34

Safu ya 2
a Kut 20:12
Kum 5:16
Efe 6:1
Kol 3:20
b Mwa 37:11
Da 7:28
Lu 2:19
c Met 2:2
Met 2:5
Isa 11:2
d Met 3:4

SURA 3
e Mt 14:1
Lu 23:7
f Mt 26:57
Yoh 18:13
Yoh 18:24
Mdo 4:6
g Yoh 1:6
h Lu 1:80
i Mt 3:1
Mk 1:4
Lu 1:77
Mdo 13:24
j Isa 40:3
Mt 3:3
Mk 1:3
k Isa 40:4
l Zb 98:2
Isa 40:5
Isa 52:10
Lu 2:30
Mdo 28:28
m Isa 59:5

51 Naye akashuka kwenda
pamoja nao mpaka Nazare-
ti, naye akaendelea kujitiisha[a]
kwao. Pia, mama yake akawe-
ka kwa uangalifu maneno yote
hayo moyoni mwake.[b] **52** Na
Yesu akazidi kufanya maende-
leo katika hekima[c] na ukuzi
wa kimwili, akipata kibali kwa
Mungu na wanadamu.[d]

3 Katika mwaka wa kumi na
tano wa kumiliki kwa Kai-
sari Tiberio, Pontio Pilato ali-
pokuwa gavana wa Yudea, na
Herode[e] alipokuwa mtawala
wa wilaya ya Galilaya, laki-
ni Filipo ndugu yake aliku-
wa mtawala wa wilaya wa nchi
ya Iturea na Trakoniti, na Li-
sania alikuwa mtawala wa wi-
laya ya Abilene, **2** katika
siku za mkuu wa makuhani
Anasi na za Kayafa,[f] tangazo la
Mungu likamjia Yohana[g] mwa-
na wa Zekaria nyikani.[h]
3 Basi akaingia katika nchi
yote kuzunguka Yordani, aki-
hubiri ubatizo unaoonyesha
toba kwa ajili ya msamaha wa
dhambi,[i] **4** kama ilivyoandi-
kwa katika kitabu cha mane-
no ya nabii Isaya: "Sikilizeni!
Mtu fulani anapaaza sauti nyi-
kani, 'Tayarisheni njia ya Yeho-
va, nyoosheni barabara zake.[j]
5 Kila mtaro lazima ujazwe,
na kila mlima na kilima vifa-
nywe tambarare, palipopindi-
ka lazima pawe njia nyoofu na
mahali penye miparuzo pawe
njia laini;[k] **6** na wote wenye
mwili wataona njia ya Mungu
ya kuokoa.' "[l]
7 Kwa hiyo akaanza kuua-
mbia umati wa watu waliokuwa
wakija awabatize: "Ninyi
uzao wa nyoka-vipiri,[m] ni nani

ambaye amewaonyesha ninyi
kuikimbia ghadhabu inayo-
kuja?[a] **8** Basi zaeni matunda
yanayofaa toba.[b] Wala msianze
kusema ndani yenu wenyewe,
'Abrahamu ndiye baba yetu.'
Kwa maana ninawaambia ni-
nyi kwamba Mungu ana nguvu
za kumwinulia Abrahamu wa-
toto kutoka katika mawe haya.
9 Kwa kweli, tayari shoka li-
mewekwa kwenye mzizi wa
miti; kwa hiyo, kila mti usi-
ozaa matunda mazuri unapa-
swa kukatwa na kutupwa nda-
ni ya moto."[c]

10 Na umati ukamuuliza:
"Basi, tufanye nini?"[d] **11** Aka-
wajibu, akawaambia: "Mtu aliye
na mavazi mawili ya ndani na
ashiriki pamoja na mtu amba-
ye hana hata moja, na aliye na
vyakula afanye vivyo hivyo."[e]
12 Lakini hata wakusanya-
kodi wakaja ili kubatizwa, nao
wakamwambia: "Mwalimu, tu-
fanye nini?"[f] **13** Akawaam-
bia: "Msidai zaidi ya kiwango
cha kodi."[g] **14** Pia, wale walio
katika utumishi wa kijeshi wa-
kamuuliza: "Na sisi pia tufanye
nini?" Naye akawaambia: "Msi-
msumbue mtu yeyote wala ku-
mshtaki[h] mtu yeyote kwa uwo-
ngo, bali mtosheke na posho
lenu."[i]

15 Basi kwa kuwa watu wa-
likuwa wakitarajia na wote
walikuwa wakiwaza mioyoni
mwao juu ya Yohana: "Je, la-
bda yeye ndiye Kristo?"[j]
16 Yohana akajibu, akawaam-
bia wote: "Mimi ninawabati-
za ninyi kwa maji; lakini mwe-
nye nguvu kuliko mimi ana-
kuja, ambaye kamba ya viatu
vyake mimi sistahili kuifu-
ngua.[a] Yeye atawabatiza ninyi
kwa roho takatifu na moto.[b]
17 Sepetu yake ya kupepetea
imo mkononi mwake ili kuusa-
fisha kabisa uwanja wake wa
kupuria na kukusanya[c] ngano
ndani ya ghala lake, lakini ma-
kapi[d] atayateketeza kwa moto[e]
usioweza kuzimwa."

18 Kwa hiyo alitoa pia ma-
himizo mengine mengi na kue-
ndelea kuwatangazia watu ha-
bari njema. **19** Lakini kwa
kuwa alikuwa amemkaripia
Herode mtawala wa wilaya ku-
husu Herodia mke wa ndu-
gu yake na kuhusu matendo
yote maovu ambayo Herode
alikuwa amefanya,[f] **20** alio-
ngeza hili pia kwa matendo
yote hayo: alimfungia Yohana
gerezani.[g]

21 Basi watu wote walipo-
kuwa wamebatizwa, Yesu[h] pia
akabatizwa na, alipokuwa
akisali, mbingu[i] ilifunguli-
wa **22** na roho takatifu kati-
ka umbo la njiwa ikashuka juu
yake, na sauti ikatoka mbingu-
ni: "Wewe ni Mwanangu, mpe-
ndwa; nimekukubali wewe."[j]

23 Tena, Yesu mwenyewe,
alipoanza kazi yake,[k] alikuwa
na umri wa karibu miaka 30,[l]
akiwa mwana,[m] kama alivyoo-
nwa,

wa Yosefu,[n]
mwana wa Heli,
24 mwana wa Mathati,
mwana wa Lawi,
mwana wa Melki,
mwana wa Yanai,
mwana wa Yosefu,
25 mwana wa Matathia,
mwana wa Amosi,
mwana wa Nahumu,
mwana wa Esli,
mwana wa Nagai,

SURA 3
a Mt 3:7
Mt 23:33
b Mt 3:8
Mdo 26:20
c Mt 3:10
Mt 7:19
Yoh 15:6
d Mdo 2:37
Mdo 16:30
e Mdo 10:2
2Ko 8:14
1Ti 6:18
Yak 2:15
1Yo 3:17
f Mt 21:32
Lu 7:29
g Lu 19:8
1Ko 6:10
h Kut 23:1
Kut 23:7
Law 19:11
Met 6:19
i 1Ti 6:8
j Yoh 1:25

Safu ya 2
a Mk 1:7
Mdo 13:25
b Mt 3:11
Mk 1:8
Mdo 2:4
c Mik 4:12
d Zb 1:4
e Mt 13:30
f Mt 14:3
g Mk 6:17
h Mt 3:13
Mk 1:9
i Mt 3:16
Mk 1:10
j Zb 2:7
Mt 3:17
Mk 1:11
Yoh 1:32
2Pe 1:17
k Mdo 10:38
l Hes 4:3
m Mt 13:55
n Mt 1:16
Lu 1:35
Lu 4:22
Yoh 6:42

26 mwana wa Maathi,
mwana wa Matathia,
mwana wa Semei,
mwana wa Yoseki,
mwana wa Yoda,
27 mwana wa Yoanani,
mwana wa Resa,
mwana wa Zerubabeli,[a]
mwana wa Shealtieli,[b]
mwana wa Neri,
28 mwana wa Melki,
mwana wa Adi,
mwana wa Kosamu,
mwana wa Elmadamu,
mwana wa Eri,
29 mwana wa Yesu,
mwana wa Eliezeri,
mwana wa Yorimu,
mwana wa Mathati,
mwana wa Lawi,
30 mwana wa Simioni,
mwana wa Yuda,
mwana wa Yosefu,
mwana wa Yonamu,
mwana wa Eliakimu,
31 mwana wa Melea,
mwana wa Mena,
mwana wa Matatha,
mwana wa Nathani,[c]
mwana wa Daudi,[d]
32 mwana wa Yese,[e]
mwana wa Obedi,[f]
mwana wa Boazi,[g]
mwana wa Salmoni,[h]
mwana wa Nashoni,[i]
33 mwana wa Aminadabu,[j]
mwana wa Arni,[k]
mwana wa Hezroni,[l]
mwana wa Perezi,[m]
mwana wa Yuda,[n]
34 mwana wa Yakobo,[o]
mwana wa Isaka,[p]
mwana wa Abrahamu,[q]
mwana wa Tera,[r]
mwana wa Nahori,[s]
35 mwana wa Serugi,[t]
mwana wa Reu,[u]
mwana wa Pelegi,[v]
mwana wa Eberi,[a]
mwana wa Shela,[b]
36 mwana wa Kainani,
mwana wa Arpakshadi,[c]
mwana wa Shemu,[d]
mwana wa Noa,[e]
mwana wa Lameki,[f]
37 mwana wa Methusela,[g]
mwana wa Enoko,[h]
mwana wa Yaredi,[i]
mwana wa Mahalaleeli,[j]
mwana wa Kainani,[k]
38 mwana wa Enoshi,[l]
mwana wa Sethi,[m]
mwana wa Adamu,[n]
mwana wa Mungu.

4 Basi Yesu, akiwa amejaa roho takatifu, akarudi kutoka Yordani, naye akaongozwa na roho huku na huku nyikani[o] **2** kwa siku 40,[p] alipokuwa akijaribiwa[q] na Ibilisi. Zaidi ya hayo, hakula chochote katika siku hizo, na kwa hiyo, zilipomalizika, akaona njaa. **3** Ndipo Ibilisi akamwambia: "Ikiwa wewe ni mwana wa Mungu, liambie jiwe hili liwe mkate." **4** Lakini Yesu akamjibu: "Imeandikwa, 'Mwanadamu hataishi kwa mkate tu.'"[r]

5 Kwa hiyo akamleta juu na kumwonyesha mara moja falme zote za dunia inayokaliwa; **6** naye Ibilisi akamwambia: "Hakika nitakupa mamlaka[s] yote hii na utukufu wake, kwa sababu nimepewa, na yeyote ninayetaka mimi humpa.[t] **7** Kwa hiyo, ukifanya tendo[u] la ibada mbele yangu, yote itakuwa yako." **8** Yesu akajibu akamwambia: "Imeandikwa, 'Yehova Mungu[v] wako ndiye unayepaswa kumwabudu, na yeye peke yake ndiye unayepaswa kumtolea utumishi mtakatifu.'"[w]

SURA 3

a Ezr 3:2
b 1Nya 3:17
Mt 1:12
c 2Sa 5:14
d 1Sa 16:13
1Nya 3:5
Mt 1:6
e 1Sa 17:58
Isa 11:1
Mt 1:6
f Ru 4:17
g Ru 4:13
h Ru 4:21
Mt 1:5
i Hes 1:7
1Nya 2:11
Mt 1:4
j Ru 4:20
k 1Nya 2:10
l Ru 4:19
m Ru 4:18
1Nya 2:5
n Mwa 29:35
Ru 4:12
1Nya 2:4
Mt 1:3
o Mwa 25:26
1Nya 2:1
p Mwa 21:3
q Mwa 11:27
1Nya 1:28
Mt 1:2
r Mwa 11:26
s Mwa 11:24
t Mwa 11:22
u Mwa 11:20
1Nya 1:25
v Mwa 11:18

Safu ya 2

a Mwa 11:16
b Mwa 11:14
c Mwa 11:12
d Mwa 11:10
e Mwa 5:29
Mwa 5:32
f Mwa 5:25
g Mwa 5:21
h Mwa 5:19
i Mwa 5:16
j Mwa 5:12
k Mwa 5:9
1Nya 1:2
l Mwa 4:26
Mwa 5:7
Mwa 5:10
1Nya 1:1
m Mwa 5:4
n Mwa 5:1

SURA 4

o Law 16:21
Mt 4:1
Mk 1:12
p Kut 34:28
1Fa 19:8
q Ebr 2:18
r Kum 8:3
s Ufu 13:2
t Yoh 12:31
Yoh 14:30
Efe 2:2
u Da 3:5
v Kut 20:3
w Kum 6:13
Kum 10:20

9 Sasa akamwongoza kuingia Yerusalemu, akamsimamisha juu ya mnara[a] wa hekalu na kumwambia: "Ikiwa wewe ni mwana wa Mungu, jitupe chini kutoka hapa;[b] **10** kwa maana imeandikwa, 'Atawaagiza malaika zake kukuhusu wewe, ili wakulinde,'[c] **11** nao, 'Watakuchukua mikononi mwao, ili usipate kamwe kuugonga mguu wako juu ya jiwe.'"[d] **12** Yesu akajibu, akamwambia: "Imesemwa, 'Usimjaribu Yehova Mungu wako.'"[e] **13** Kwa hiyo Ibilisi, akiisha kumaliza majaribu yote, akamwacha mpaka wakati mwingine unaofaa.[f]

14 Basi Yesu akarudi katika nguvu za roho na kuingia Galilaya.[g] Na habari nzuri juu yake zikaenea katika nchi yote inayozunguka.[h] **15** Pia, akaanza kufundisha katika masinagogi yao, akiheshimiwa na wote.[i]

16 Naye akaja mpaka Nazareti,[j] ambako alikuwa amelelewa; na, kulingana na desturi yake siku ya sabato, akaingia katika sinagogi,[k] naye akasimama ili asome. **17** Kwa hiyo akapewa kitabu cha kukunjwa cha nabii Isaya, naye akakifungua na kupata mahali palipokuwa pameandikwa: **18** "Roho ya Yehova[l] iko juu yangu, kwa sababu alinitia mafuta kuwatangazia maskini habari njema, alituma kuhubiri kuachiliwa huru kwa mateka na kupata kuona tena kwa vipofu, kuacha waliopondeka waende zao wakiwa wameachiliwa huru,[m] **19** kuhubiri mwaka wa Yehova wenye kukubalika."[n] **20** Ndipo akakikunja kitabu hicho, akamrudishia mtumishi, akaketi; na wote katika sinagogi wakamkazia macho. **21** Ndipo akaanza kuwaambia: "Leo andiko hili ambalo mmesikia sasa hivi limetimizwa."[a]

22 Nao wote wakaanza kutoa ushahidi mwema juu yake wakistaajabia maneno yenye kuvutia[b] sana yaliyokuwa yakitoka kinywani mwake, na walikuwa wakisema: "Huyu ni mwana wa Yosefu, sivyo?"[c] **23** Ndipo akawaambia: "Bila shaka mtautumia mfano huu kwangu, 'Tabibu,[d] jiponye mwenyewe; mambo[e] tuliyosikia kwamba yamekwisha kutukia katika Kapernaumu[f] yafanye pia hapa katika eneo la nyumbani kwako.'"[g] **24** Lakini akawaambia: "Kwa kweli ninawaambia ninyi kwamba hakuna nabii anayekubaliwa katika eneo la nyumbani kwake. **25** Kwa mfano, kwa kweli ninawaambia ninyi, Kulikuwa na wajane wengi katika Israeli siku za Eliya, wakati mbingu ilipofungwa kwa miaka mitatu na miezi sita, hivi kwamba njaa kubwa ikatokea katika nchi yote,[h] **26** lakini Eliya hakutumwa kwenda kwa hata mmoja wa wanawake hao, ila tu kwenda Sarefathi[i] katika nchi ya Sidoni kwa mjane mmoja. **27** Pia, kulikuwa na wenye ukoma wengi katika Israeli wakati wa nabii Elisha, lakini hakuna hata mmoja wao aliyetakaswa, ila Naamani yule mtu wa Siria."[j] **28** Basi wote hao waliokuwa wakisikia mambo hayo katika sinagogi wakajawa na hasira;[k] **29** nao wakaondoka,

SURA 4

a Mt 4:5
b Mt 4:6
c Zb 91:11
d Zb 91:12
e Kum 6:16
1Ko 10:9
f Ebr 4:15
g Mt 4:12
Yoh 4:3
h Mdo 10:37
i Isa 52:13
j Mt 2:23
k Mdo 13:14
Mdo 17:2
l Isa 61:1
m Isa 42:3
Mt 12:20
n Isa 58:6
Isa 61:2

Safu ya 2

a Mt 5:17
2Ko 6:2
b Zb 45:2
Isa 50:4
Efe 4:29
c Mt 13:54
Mk 6:2
Yoh 6:42
d Mt 8:7
e Mt 9:12
f Mt 4:13
g Mt 13:57
Mk 6:4
Yoh 4:44
h 1Fa 17:9
1Fa 18:1
Yak 5:17
i 1Fa 17:10
j 2Fa 5:14
k Lu 2:34

wakamharakisha kwenda nje
ya jiji, nao wakampeleka mpa-
ka ukingo wa mlima ambao
jiji lao lilikuwa limejengwa juu
yake, ili wamporomoshe chini.[a]
30 Lakini akapita katikati yao
na kwenda zake.[b]
31 Naye akashuka kwenda
Kapernaumu,[c] jiji moja la
Galilaya. Naye alikuwa aki-
wafundisha siku ya sabato;
32 nao wakastaajabishwa na
njia yake ya kufundisha,[d] kwa
sababu maneno yake yaliku-
wa yenye mamlaka.[e] **33** Basi
katika sinagogi kulikuwa na
mtu mwenye roho,[f] roho mwo-
vu, mchafu, naye akapaaza sa-
uti: **34** "Ah! Tuna nini nawe,[g]
Yesu Mnazareti?[h] Je, umekuja
kutuangamiza? Ninajua[i] wewe
ni nani, Mtakatifu wa Mungu."[j]
35 Lakini Yesu akamkemea,
akisema: "Nyamaza, na umto-
ke." Kwa hiyo, baada ya ku-
mwangusha mtu huyo chini
katikati yao, yule roho mwovu
akamtoka bila kumuumiza.[k]
36 Ndipo wote wakashangaa,
nao wakaanza kuongea wao
kwa wao, wakisema: "Maneno
haya ni ya namna gani, kwa
sababu yeye huagiza roho wa-
chafu kwa mamlaka na nguvu,
nao hutoka?"[l] **37** Kwa hiyo
habari juu yake zikaenea kati-
ka kila pembe ya nchi yenye
kuzunguka.[m]
38 Baada ya kutoka katika
sinagogi akaingia katika nyu-
mba ya Simoni. Basi mama-
mkwe wa Simoni alikuwa aki-
taabishwa na homa kali, nao
wakamwomba Yesu kwa ajili
yake.[n] **39** Kwa hiyo akasi-
mama kando yake akaikemea
homa hiyo,[o] nayo ikamwacha.
Akasimama mara moja akaa-
nza kuwahudumia.[a]
40 Lakini jua lilipokuwa li-
kitua, wale wote waliokuwa
na watu wanaougua mago-
njwa mbalimbali wakawale-
ta kwake. Akawa akiwaponya
kwa kuweka mikono yake juu
ya kila mmoja wao.[b] **41** Roho
waovu pia wakawa wakiwato-
ka wengi,[c] wakipaaza sauti na
kusema: "Wewe ndiye Mwana
wa Mungu."[d] Lakini, kwa ku-
wakemea, hakuwa akiwaruhu-
su kusema,[e] kwa sababu wali-
jua kuwa yeye[f] ndiye Kristo.[g]
42 Hata hivyo, kulipoku-
wa mchana, akaenda mahali
ambapo hapakuwa na watu.[h]
Lakini umati ukaanza kumta-
futa huku na huku na kuja
mpaka alipokuwa, nao ukaja-
ribu kumzuia asitoke kwao.
43 Lakini akawaambia: "Ni la-
zima nitangaze habari njema
ya ufalme wa Mungu kwenye
majiji mengine pia, kwa saba-
bu nilitumwa kufanya hivyo."[i]
44 Basi akaendelea kuhubiri
katika masinagogi ya Yudea.[j]

5 Pindi moja umati ulipo-
kuwa ukimsonga na ku-
sikiliza neno la Mungu, ali-
kuwa amesimama kando ya
ziwa la Genesareti.[k] **2** Naye
akaona mashua mbili zimeege-
shwa kando ya ziwa, lakini wa-
vuvi walikuwa wametoka nda-
ni yake nao walikuwa wakio-
sha nyavu zao.[l] **3** Akapanda
ndani ya moja kati ya mashua
hizo, iliyokuwa ya Simoni, aka-
mwomba aivute mbali kido-
go na nchi kavu. Ndipo aka-
keti, na kuanza kuufundisha
umati akiwa kwenye mashua[m]
hiyo. **4** Alipoacha kusema,

SURA 4
a Mt 21:38
b Yoh 8:59
Yoh 10:39
c Mk 1:21
d Mt 7:28
Yoh 7:46
e Tit 2:15
f Mk 1:23
g Mt 8:29
Lu 8:28
h Mt 2:23
Lu 18:37
Yoh 19:19
Mdo 2:22
i Yak 2:19
j Mk 1:24
Lu 1:35
Lu 4:41
akasimama[h] na kuanza kusa-
li[i] mambo haya akisema mo-
yoni, 'Ee Mungu, ninakushu-
kuru ya kuwa mimi si kama
wale watu wengine, wanya-
ng'anyi, wasio waadilifu, wazi-
nzi, au hata kama mkusanya-
kodi huyu.[j] **12** Mimi hufunga
mara mbili kwa juma, mimi
hutoa sehemu ya kumi ya
vitu vyote ninavyojipatia.'[k]
13 Lakini yule mkusanya-
kodi akiwa amesimama umba-
li fulani hakutaka hata kui-
nua macho yake kuelekea mbi-
nguni, bali alikuwa akipiga-
piga kifua chake,[a] akisema, 'Ee
Mungu, unirehemu mimi mte-
nda-dhambi.'[b] **14** Ninawaa-
mbia ninyi, Mtu huyu alishuka
kwenda nyumbani kwake aki-
wa amethibitishwa kuwa mwa-
dilifu[c] zaidi kuliko yule mwi-
ngine; kwa sababu kila mtu
anayejiinua atafedheheshwa,
bali yule anayejinyenyekeza
atainuliwa."[d]

15 Sasa watu wakaanza ku-
mletea pia watoto wao wacha-
nga ili awaguse; lakini walipo-
na hilo wanafunzi wakaanza
kuwakemea.[e] **16** Hata hivyo,
Yesu akawaita wale watoto, aki-
sema: "Waacheni watoto wa-
changa waje kwangu, wala msi-
jaribu kuwazuia. Kwa maana
ufalme wa Mungu ni wa wale
walio kama hao.[f] **17** Kwa
kweli ninawaambia ninyi, Mtu
yeyote ambaye haupokei ufa-
lme wa Mungu kama mtoto
mchanga hataingia kamwe nda-
ni yake."[g]

18 Na mtawala fulani aka-
muuliza, akisema: "Mwali-
mu Mwema, nifanye nini ili
niurithi uzima wa milele?"[h]
19 Yesu akamwambia: "Kwa
nini unaniita mwema? Hakuna
mtu aliye mwema, ila mmoja,
Mungu.[i] **20** Wewe unazijua
amri,[j] 'Usifanye uzinzi,[k] Usiue,[l]
Usiibe,[m] Usitoe ushahidi wa
uwongo,[n] Mheshimu baba yako
na mama yako.'"[o] **21** Ndipo
akasema: "Yote hayo nime-
yashika tangu ujana wangu
na kuendelea."[p] **22** Baada ya
kusikia hilo, Yesu akamwa-
mbia: "Bado kuna jambo moja
unalokosa: Uza vitu vyote uli-
vyo navyo uwagawie maskini,
nawe utakuwa na hazina mbi-

SURA 18
a Lu 11:7
b Amu 16:16
c 1Sa 24:12
Isa 40:27
Yer 20:12
d 2Pe 3:9
Ufu 6:10
e Hab 2:3
Ebr 10:37
f Met 30:12
Lu 10:29
g Isa 65:5
h Zb 135:2
i Isa 1:15
j Ufu 3:17
k Mt 23:23

Safu ya 2
a Yer 31:19
Lu 23:48
b Zb 51:3
c 1Sa 16:7
Isa 66:2
Mt 21:31
d Isa 2:11
Mt 23:12
Yak 4:6
1Pe 5:5
e Mt 19:13
Mk 10:13
f 1Ko 14:20
1Pe 2:2
g Mt 18:3
Mk 10:15
h Mt 19:16
Mk 10:17
Lu 10:25
i Mt 19:17
Mk 10:18
j Ro 13:9
k Kut 20:14
Kum 5:18
l Kut 20:13
Kum 5:17
m Kut 20:15
Kum 5:19
n Kut 20:16
Kum 5:20
o Kut 20:12
Kum 5:16
Efe 6:2
p Mt 19:20
Mk 10:20

nguni; kisha uje uwe mfuasi
wangu."[a] **23** Aliposikia neno
hilo, akahuzunika sana, kwa
maana alikuwa tajiri sana.[b]
24 Yesu akamtazama na ku-
sema: "Jinsi itakavyokuwa vi-
gumu kwa wale walio na pesa
kuingia katika ufalme wa Mu-
ngu![c] **25** Kwa kweli, ni rahi-
si zaidi ngamia kupita kati-
ka tundu la sindano ya ku-
shonea kuliko tajiri kuingia
katika ufalme wa Mungu."[d]
26 Wale waliosikia hilo wa-
kasema: "Ni nani anayewe-
za kuokolewa?" **27** Akase-
ma: "Mambo yasiyowezekana
kwa wanadamu yanawezeka-
na kwa Mungu."[e] **28** Laki-
ni Petro akasema: "Tazama!
Tumeacha vitu vyetu we-
nyewe na kukufuata wewe."[f]
29 Akawaambia: "Kwa kwe-
li ninawaambia ninyi, Hakuna
yeyote ambaye ameacha nyu-
mba au mke au ndugu au waza-
zi au watoto kwa ajili ya ufalme
wa Mungu[g] **30** ambaye hata-
pata mara nyingi zaidi katika
kipindi hiki cha wakati, na ka-
tika mfumo wa mambo unao-
kuja uzima wa milele."[h]
31 Ndipo akawachukua
wale kumi na wawili kando
na kuwaambia: "Tazameni! Tu-
napanda kwenda Yerusalemu,
na mambo yote yaliyoandikwa
kupitia manabii[i] juu ya Mwa-
na wa binadamu yatatimia.[j]
32 Kwa mfano, atatiwa mi-
kononi mwa watu wa mataifa
naye atadhihakiwa[k] na ku-
tendewa kwa dharau[l] na ku-
temewa mate;[m] **33** na baada
ya kumpiga mijeledi[n] wata-
muua,[o] lakini katika siku ya
tatu atafufuka."[p] **34** Hata hi-

SURA 18

a Mt 6:20
Mt 19:21
Mk 10:21
Lu 12:33
1Ti 6:19
b Mt 19:22
Mk 10:22
c Met 11:28
Mt 19:23
1Ti 6:9
d Mt 19:24
Mk 10:25
e Mwa 18:14
Yer 32:17
Zek 8:6
Mk 14:36
f Mt 19:27
g Kum 33:9
Mk 10:29
h Mt 19:29
Mk 10:30
Ufu 2:10
i Zb 16:10
Zb 22:Uta-
31
Zb 34:20
Zb 41:9
Zb 69:21
Isa 53:1-12
Mik 5:1
Zek 9:9
Zek 11:12
Zek 13:7
j Mt 16:21
Mk 10:32
k Zb 22:7
Mt 27:2
Mdo 3:13
l Isa 53:5
m Isa 50:6
n Isa 53:5
o Isa 53:7
p Yon 1:17
Mt 20:19
Mk 10:34
Lu 9:22

Safu ya 2

a Mk 9:32
Yoh 10:6
b Mt 20:29
Mk 10:46
c Mk 10:47
d Mt 20:30
Lu 17:13
e Mt 20:31
Mk 10:48
f Mk 10:49
g Mt 20:32
h Mt 20:33
Mk 10:51
i Mt 20:34
Lu 7:50
Lu 17:19
j Mk 10:52
k Lu 5:26
Mdo 4:21
Ga 1:24

SURA 19

l Mt 20:29
m Yoh 6:24
Yoh 12:21

vyo, wao hawakupata maana
ya lolote kati ya mambo hayo;
lakini walikuwa wamefichwa
maneno hayo, nao hawakujua
mambo yaliyosemwa.[a]
35 Sasa alipokuwa akikari-
bia Yeriko mtu fulani aliye ki-
pofu alikuwa ameketi kando
ya barabara akiombaomba.[b]
36 Kwa sababu aliusikia uma-
ti ukipita, akaanza kuuliza ma-
ana ya mambo hayo. **37** Wa-
kamwambia: "Yesu Mnazare-
ti anapitia hapa!"[c] **38** Ndipo
akapaaza sauti, akisema: "Yesu,
Mwana wa Daudi, unireheu-
mu!"[d] **39** Na wale waliokuwa
mbele wakaanza kumwam-
bia kwa kusisitiza anyama-
ze, lakini ndivyo naye alivyo-
zidi kupaaza sauti: "Mwana wa
Daudi, unirehemu."[e] **40** Ndi-
po Yesu akasimama tuli na ku-
amuru mtu huyo aletwe kwa-
ke.[f] Alipokaribia, Yesu akamu-
uliza: **41** "Unataka nikufa-
nyie nini?"[g] Akasema: "Bwana,
acha nipate kuona tena."[h]
42 Kwa hiyo Yesu akamwam-
bia: "Ona tena; imani yako
imekuponya."[i] **43** Na mara
moja akapata kuona tena,[j]
naye akaanza kumfuata, aki-
mtukuza Mungu.[k] Pia, watu
wote, walipoona hilo, waka-
msifu Mungu.

19 Naye akaingia Yeriko[l] na
akawa akipita. **2** Sasa
kulikuwa na mwanamume ana-
yeitwa Zakayo; naye alikuwa
mkuu wa wakusanya-kodi, na
alikuwa tajiri. **3** Basi, aliku-
wa akitafuta kuona[m] Yesu
huyu ni nani, lakini hange-
weza kwa sababu ya umati,
kwa sababu alikuwa mfupi.
4 Kwa hiyo akakimbia mbele

na kupanda mforsadi-tini ku-
sudi amwone, kwa sababu ali-
kuwa karibu kupitia njia hiyo.
5 Sasa Yesu alipofika hapo,
akatazama juu na kumwambia:
"Zakayo, shuka haraka, kwa
maana leo lazima nikae ka-
tika nyumba yako." **6** Ndipo
akafanya haraka, akashuka,
akamkaribisha kwa shangwe.
7 Lakini walipoona hilo, wote
wakaanza kunung'unika,[a] wa-
kisema: "Ameingia apate ku-
kaa pamoja na mwanamume
mtenda-dhambi." **8** Lakini
Zakayo akasimama na kumwa-
mbia Bwana: "Tazama! Nusu ya
mali zangu, Bwana, mimi nita-
wapa maskini, na chochote ni-
lichomnyang'anya mtu yeyo-
te kwa shtaka la uwongo[b] ni-
tarudisha mara nne."[c] **9** Ndi-
po Yesu akamwambia: "Leo
wokovu umekuja kwenye nyu-
mba hii, kwa sababu yeye
pia ni mwana wa Abrahamu.[d]
10 Kwa maana Mwana wa bi-
nadamu alikuja kutafuta na
kuokoa kilichopotea."[e]

11 Walipokuwa wakisikili-
za mambo hayo akatoa mfa-
no kwa kuongezea, kwa sa-
babu alikuwa karibu na Yeru-
salemu nao walikuwa wakiwa-
zia kwamba ufalme wa Mungu
ulikuwa ukikaribia kujionye-
sha mara moja.[f] **12** Kwa hiyo
akasema: "Mtu fulani wa ukoo
mashuhuri alisafiri mpaka nchi
ya mbali ili ajipatie mamlaka
ya kifalme kwa ajili yake mwe-
nyewe na kurudi.[g] **13** Akai-
ta kumi kati ya watumwa
wake akawapa mina kumi na
kuwaambia, 'Fanyeni biasha-
ra mpaka nije.'[h] **14** Lakini
raia zake wakamchukia[i] na ku-
tuma baraza la mabalozi ku-
mfuata, na kusema, 'Hatumta-
ki mtu huyu awe mfalme juu
yetu.'[a]

15 "Mwishowe aliporudi ba-
ada ya kupata mamlaka ya ki-
falme aliamuru watumwa hao
ambao alikuwa amewapa fe-
dha waitwe, ili ahakikishe kile
walichokuwa wamepata faida
kwa biashara.[b] **16** Ndipo wa
kwanza akajitokeza, akisema,
'Bwana, mina yako ilipata faida
ya mina kumi.'[c] **17** Kwa hiyo
akamwambia, 'Vema, mtumwa
mwema! Kwa sababu katika ja-
mbo dogo sana umejionyesha
mwenyewe kuwa mwaminifu,
uwe na mamlaka juu ya maji-
ji kumi.'[d] **18** Sasa wa pili aka-
ja, akisema, 'Mina yako, Bwana,
ilileta mina tano.'[e] **19** Aka-
mwambia huyu pia, 'Wewe, pia,
usimamie majiji matano.'[f]
20 Lakini mwingine akaja, aki-
sema, 'Bwana, hii hapa mina
yako, ambayo niliitunza ikiwa
imehifadhiwa katika kita-
mbaa. **21** Unaona, nilikuogo-
pa, kwa sababu wewe ni mtu
mgumu; wewe huchukua kile
ambacho hukuweka akiba
nawe huvuna kile ambacho
hukupanda.'[g] **22** Akamwa-
mbia, 'Ninakuhukumu kutoka
kinywani mwako mwenyewe,[h]
mtumwa mwovu. Ulijua, sivyo,
kwamba mimi ni mtu mgumu,
ambaye huchukua kile amba-
cho sikuweka akiba na kuvu-
na kile ambacho sikupanda?[i]
23 Kwa hiyo kwa nini hukutia
fedha zangu katika mahali pa
kutunzia akiba? Kisha wakati
ambapo ningefika ningezichu-
kua pamoja na faida.'[j]

SURA 19

a Mt 9:11
Lu 5:30
Lu 15:2

b Kut 20:16
Lu 3:14

c Kut 22:1
Law 6:5
2Sa 12:6

d Mt 15:24
Lu 13:16
Mdo 3:25

e Eze 34:16
Mt 9:13
Mt 10:6
Lu 15:4
Ro 5:8
1Ti 1:15

f Mt 24:33
Lu 17:20
Mdo 1:6
2Th 2:2

g Mt 25:14
Mk 13:34
Yoh 18:36

h Mt 25:15

i Yoh 1:11

Safu ya 2

a Zb 2:2
Mt 23:37

b Mt 25:19

c Mt 25:20

d Mt 25:21
Lu 16:10
Ufu 2:26

e Mt 25:22

f Mt 25:23

g Mt 25:24

h 2Sa 1:16
Mt 12:37

i Mt 25:26

j Kum 23:20
Mt 25:27

24 "Ndipo akawaambia wale
waliokuwa wamesimama ka-
ndo, 'Chukueni hiyo mina ku-
toka kwake mkampe yule ali-
ye na mina kumi.'[a] **25** Lakini
wakamwambia, 'Bwana, huyo
ana mina kumi!'— **26** 'Nina-
waambia ninyi, Kila mtu ali-
ye na kitu, ataongezewa; laki-
ni yule ambaye hana, hata kile
alicho nacho kitachukuliwa.[b]
27 Zaidi ya hayo, hao adui za-
ngu ambao hawakutaka niwe
mfalme juu yao waleteni hapa
mkawaue mbele yangu.'"[c]

28 Kwa hiyo, alipokuwa
amesema hayo, akaanza kwe-
nda, akipanda kwenda Yerusa-
lemu.[d] **29** Naye alipokaribia
Bethfage na Bethania kwenye
mlima unaoitwa Mlima wa Mi-
zeituni,[e] akatuma wawili kati
ya wanafunzi,[f] **30** akisema:
"Nendeni mkaingie katika kiji-
ji mnachokiona mbele yenu,
na ndani yake baada ya kui-
ngia mtamkuta mwana-punda
akiwa amefungwa, ambaye ha-
kuna yeyote kati ya wanadamu
ambaye amewahi kuketi juu
yake. Mfungueni mkamlete.[g]
31 Lakini mtu yeyote akiwau-
liza ninyi, 'Kwa nini mnamfu-
ngua?' Mwambieni hivi, 'Bwa-
na anamhitaji.'"[h] **32** Kwa
hiyo wale waliotumwa wakao-
ndoka wakakuta sawa na vile
alivyowaambia.[i] **33** Lakini
walipokuwa wakimfungua
mwana-punda, wenyewe waka-
waambia: "Kwa nini mnamfu-
ngua huyo mwana-punda?"[j]
34 Wakasema: "Bwana ana-
mhitaji."[k] **35** Nao wakampe-
leka kwa Yesu, nao wakayatu-
pa mavazi yao ya nje juu ya
huyo mwana-punda na kumwe-
ka Yesu juu yake.[l]

SURA 19

a Mt 25:28
b Mt 13:12
Mt 25:29
Mk 4:25
Lu 8:18
c Mwa 3:15
Zb 2:9
Isa 60:12
1Ko 15:25
2Th 1:9
Ufu 19:15
d Mk 10:32
Lu 9:51
e Yoh 8:1
Mdo 1:12
f Mt 21:1
Mk 11:1
g Mt 21:2
Mk 11:2
h Zb 50:10
Mt 21:3
Mk 11:3
i Mt 21:6
Mk 11:4
Lu 22:13
j Mk 11:5
k Mk 11:6
l 2Fa 9:13
Mt 21:7
Mk 11:7
Yoh 12:14

Safu ya 2

a Zek 9:9
b Mt 21:8
Mk 11:8
c Mt 21:9
d Isa 62:11
e Zb 118:26
Mk 11:9
Lu 2:14
f Mt 21:15
Yoh 12:19
g Hab 2:11
Mt 3:9
h Zb 119:136
Yer 9:1
Lu 23:28
Yoh 11:35
i Kum 28:52
Kum 32:29
j Isa 6:10
Mt 13:14
Mk 4:12
Mdo 28:26
Ro 11:8
k Isa 29:3
l Yer 6:6
m Lu 21:20
n Kum 28:57
Da 9:26
o Zb 137:9
Mik 3:12
Lu 23:28
p Mt 24:2
Mk 13:2
Lu 21:6
q Ho 9:7
Mik 7:4
Lu 1:68
1Pe 2:12
r Mt 21:12
Mk 11:15

36 Alipokuwa akisonga[a] mbe-
le wakawa wakitandaza ma-
vazi yao ya nje barabarani.[b]
37 Mara tu alipokaribia baraba-
ra ya kushuka Mlima wa Mi-
zeituni umati wote wa wana-
funzi wakaanza kushangilia
na kumsifu Mungu kwa sau-
ti kubwa juu ya matendo yote
yenye nguvu ambayo walikuwa
wameona,[c] **38** na kusema:
"Aliyebarikiwa ni Yule ana-
yekuja akiwa ndiye Mfalme
katika jina la Yehova![d] Amani
mbinguni, na utukufu katika
mahali palipoinuka juu zaidi!"[e]
39 Hata hivyo, baadhi
ya Mafarisayo kwenye uma-
ti wakamwambia: "Mwalimu,
wakemee wanafunzi wako."[f]
40 Lakini akajibu akasema:
"Ninawaambia ninyi, "Kama
hawa wangekaa kimya, mawe[g]
yangepaaza sauti."

41 Naye alipokaribia hapo,
akalitazama jiji na kulililia,[h]
42 akisema: "Kama wewe,
naam, wewe, ungalikuwa ume-
fahamu[i] leo mambo yanayohu-
siana na amani—lakini sasa
yamefichwa kutoka machoni
pako.[j] **43** Kwa sababu siku
zitakuja juu yako wakati adui
zako watakapojenga kukuzu-
nguka ngome[k] yenye miti iliyo-
chongoka[l] nao watakuzungu-
ka[m] na kukutaabisha[n] kutoka
kila upande, **44** nao wataku-
angusha chini wewe na wato-
to wako walio ndani yako,[o] nao
hawataacha jiwe juu ya jiwe[p]
ndani yako, kwa sababu huku-
fahamu wakati wa kukaguliwa
kwako."[q]

45 Naye akaingia katika he-
kalu na kuanza kuwafukuza
nje wale waliokuwa wakiuza,[r]

46 akiwaambia: “Imeandikwa,
‘Na nyumba yangu itakuwa
nyumba ya sala,’[a] lakini ninyi
mmeifanya kuwa pango la wa-
nyang’anyi.”[b]
47 Zaidi ya hayo, akawa aki-
fundisha kila siku katika he-
kalu. Lakini wakuu wa ma-
kuhani na waandishi na wa-
kuu kati ya watu walikuwa
wakitafuta kumwangamiza;[c]
48 na bado hawakufanikiwa,
kwa maana watu wote waliku-
wa wakishikamana sana naye
ili wamsikie.[d]

20 Siku moja alipokuwa
akifundisha watu kati-
ka hekalu na kutangaza ha-
bari njema, wakuu wa maku-
hani na waandishi pamoja na
wanaume wazee wakaja kari-
bu,[e] **2** nao wakasema, waki-
mwambia: “Tuambie unafa-
nya mambo haya kwa mamla-
ka gani, au ni nani aliyekupa
mamlaka hiyo.”[f] **3** Akajibu,
akawaambia: “Mimi pia nita-
wauliza ninyi swali, nanyi mni-
ambie:[g] **4** Je, ubatizo wa Yo-
hana ulitoka mbinguni au kwa
wanadamu?”[h] **5** Ndipo kati
yao wenyewe wakafikia kau-
li, wakisema: “Tukisema, ‘Uli-
toka mbinguni,’ atasema,
‘Kwa nini hamkumwamini?’[i]
6 Lakini tukisema, ‘Ulitoka
kwa wanadamu,’ watu wote
watatupiga kwa mawe,[j] kwa
maana wao wamesadikishwa
kwamba Yohana[k] alikuwa na-
bii.”[l] **7** Kwa hiyo wakajibu
kwamba hawakujua chanzo
chake. **8** Naye Yesu akawa-
ambia: “Wala mimi siwaambii
ninyi ninafanya mambo haya
kwa mamlaka gani.”[m]

SURA 19

a Isa 56:7
b Yer 7:11
Mt 21:13
Mk 11:17
Yoh 2:16
c Mk 11:18
Yoh 7:19
Yoh 18:20
d Mk 12:37
Lu 21:38

SURA 20

e Mt 21:23
f Mk 11:28
Mdo 4:7
Mdo 7:27
g Mt 21:24
Mk 11:29
h Mk 11:30
i Mt 21:25
Mk 11:31
j Mt 14:5
k Mt 11:9
Lu 7:29
l Mt 21:26
Mk 11:32
m Mt 21:27
Mk 11:33

Safu ya 2

a Zb 80:8
Wim 8:11
Isa 5:1
Yer 2:21
b Mt 21:33
Mk 12:1
c 2Fa 17:13
2Nya 36:15
d Mdo 7:52
e Mt 21:34
Mk 12:2
f 1Th 2:15
Ebr 11:36
g Mt 21:36
Mk 12:4
h Ne 9:29
i Mt 17:5
Yoh 3:16
j Mt 21:38
Mk 12:7
k Ebr 13:12
l Mdo 3:15
m Mt 21:40
n Mt 21:41
Mk 12:9
o Zb 118:22
1Pe 2:7
p Isa 28:16
Mt 21:42
Mk 12:10
q Isa 8:15
r Da 2:35
Da 2:44
s Zb 2:9
Isa 8:14
Mt 21:44

9 Ndipo akaanza kuwaa-
mbia watu mfano huu: “Mtu
alipanda shamba la mizabibu[a]
akalikodisha kwa wakulima,
naye akasafiri kwenda ng’ambo
kwa muda mrefu.[b] **10** Lakini
majira yake yalipofika akatuma
mtumwa[c] kwa wakulima,[d]
ili wampe sehemu ya matunda
ya shamba la mizabibu.[e] Hata
hivyo, wakulima hao wakamfu-
kuza akiwa mikono mitupu,[f] ba-
ada ya kumpiga sana. **11** La-
kini akatuma tena mtumwa to-
fauti kwao. Huyo pia wakampi-
ga sana na kumvunjia heshima
na kumfukuza akiwa miko-
no mitupu.[g] **12** Na bado tena
akamtuma wa tatu;[h] huyo pia
walimjeruhi na kumtupa nje.
13 Ndipo mwenye shamba la
mizabibu akasema, ‘Nitafanya
nini? Nitamtuma mwanangu
mpendwa.[i] Labda watamheshi-
mu huyu.’ **14** Wakulima wa-
lipomwona wakaanza kujadi-
liana, wakisema, ‘Huyu ndiye
mrithi; acheni tumuue, ili uri-
thi uwe wetu.’[j] **15** Ndipo wa-
kamtupa nje[k] ya shamba la mi-
zabibu na kumuua.[l] Kwa hiyo,
mwenye shamba la mizabibu
atawafanya nini?[m] **16** Ata-
kuja awaangamize wakulima
hao na kuwapa wengine sha-
mba hilo la mizabibu.”[n]
Waliposikia hilo wakasema:
“Jambo hilo lisitukie kamwe!”
17 Lakini akawatazama na
kusema: “Basi, hili ambalo li-
meandikwa humaanisha nini,
‘Jiwe ambalo wajenzi walili-
kataa,[o] limekuwa jiwe kuu la
pembeni’?[p] **18** Kila mtu ana-
yeanguka juu ya jiwe hilo
atavunjwa-vunjwa.[q] Na yeyote
ambaye litamwangukia,[r] lita-
mponda-ponda.”[s]

19 Waandishi na wakuu wa
makuhani sasa wakatafuta ku-
nyoosha mkono ili wamkama-
te saa ileile, lakini waliwaogo-
pa watu; kwa maana walifa-
hamu kwamba alisema mfano
huo juu yao.[a] **20** Na, baada
ya kumtazama sana, wakatu-
ma watu waliokodiwa kwa siri
wasingizie kwamba walikuwa
waadilifu, ili wapate kumnasa[b]
katika maneno, ili wamkabidhi
kwa serikali na kwa mamlaka
ya gavana.[c] **21** Nao wakamu-
uliza, wakisema: "Mwalimu,
tunajua wewe husema na kufu-
ndisha kwa usahihi na huonye-
shi ubaguzi wowote, bali wewe
hufundisha njia ya Mungu ku-
patana na ile kweli:[d] **22** Je,
ni halali sisi kumlipa Kaisari
kodi au hapana?"[e] **23** Lakini
akagundua ujanja wao na ku-
waambia:[f] **24** "Nionyesheni
dinari. Ina sanamu na mwandi-
ko wa nani?" Wakasema: "Wa
Kaisari."[g] **25** Akawaambia:
"Kwa vyovyote, basi, mlipeni
Kaisari vitu vya Kaisari,[h] laki-
ni mlipeni Mungu vitu vya Mu-
ngu."[i] **26** Basi, hawakuweza
kumnasa katika maneno haya
mbele ya watu, bali, wakiwa
wameshangazwa na jibu lake,
hawakusema kitu.[j]

27 Hata hivyo, baadhi ya
Masadukayo, wale ambao hu-
sema hakuna ufufuo, wakaja[k]
na kumuuliza swali, **28** wa-
kisema: "Mwalimu, Musa[l] ali-
tuandikia, 'Ndugu ya mtu aki-
fa akiwa na mke, lakini haku-
wa na mtoto, ndugu yake[m] ana-
paswa kumchukua mke huyo
na kumwinulia ndugu yake
uzao kutoka kwa mwana-
mke huyo.'[n] **29** Basi kuliku-
wa na ndugu saba; na wa kwa-
nza akamchukua mke na kufa
bila mtoto.[a] **30** Na wa pili,
31 na wa tatu, wakamchukua
mwanamke huyo. Vivyo hi-
vyo hata wa saba: hawakuacha
uzao, bali walikufa mmoja baa-
da ya mwingine.[b] **32** Mwi-
showe, yule mwanamke aka-
fa pia.[c] **33** Kwa hiyo, kati-
ka ufufuo, atakuwa mke wa
nani kati yao? Kwa maana
wale saba walimchukua kama
mke."[d]

34 Yesu akawaambia: "Wa-
toto wa mfumo huu wa mambo
huoa[e] na huolewa, **35** laki-
ni wale ambao wamehesabiwa
kustahili[f] kuupata mfumo ule
wa mambo[g] na ufufuo kuto-
ka kwa wafu[h] hawaoi wala ha-
waolewi. **36** Kwa kweli, wala
hawawezi kufa[i] tena kamwe,
kwa maana wao ni kama mala-
ika, nao ni watoto wa Mungu
kwa kuwa watoto wa ufufuo.[j]
37 Lakini hata Musa alifunua
kwamba wafu watafufuliwa,
katika masimulizi juu ya ule
mti wa miiba,[k] anapomwita Ye-
hova 'Mungu wa Abrahamu
na Mungu wa Isaka na Mungu
wa Yakobo.'[l] **38** Yeye ni Mu-
ngu, si wa wafu, bali wa wa-
lio hai, kwa maana kwake, hao
wote wako hai."[m] **39** Baadhi
ya waandishi wakajibu, wa-
kasema: "Mwalimu, umesema
vema." **40** Kwa maana ha-
wakuwa tena na ujasiri wa ku-
muuliza hata swali moja.

41 Naye akawaambia: "Kwa
nini wao husema kwamba Kri-
sto ni mwana wa Daudi?[n]
42 Kwa maana Daudi mwe-
nyewe anasema katika kita-
bu cha Zaburi, 'Yehova alimwa-
mbia Bwana wangu: "Keti kwe-
nye mkono wangu wa kuume

SURA 20
a Mt 21:45
Mk 12:12
b Lu 11:54
c Mt 22:15
Mk 12:13
d Law 19:15
Mt 22:16
Mk 12:14
e Mt 22:17
f Met 26:24
Mt 22:18
Mk 12:15
g Mt 22:20
Mk 12:16
h Ro 13:7
Tit 3:1
1Pe 2:13
i Mt 22:21
Mk 12:17
Lu 23:2
j Mt 22:22
k Mt 22:23
Mk 12:18
Mdo 23:8
l Kum 25:5
m Mwa 38:8
n Mt 22:24
Mk 12:19

Safu ya 2
a Mt 22:25
b Mk 12:21
c Mt 22:27
d Mt 22:28
Mk 12:23
e Mwa 1:28
Lu 17:27
f Ufu 3:4
g Efe 1:21
Ebr 1:2
Ebr 6:5
2Pe 3:13
h Yoh 5:29
Mdo 24:15
i Ufu 21:4
j Mt 22:30
Mk 12:25
Yoh 5:29
k Kut 3:2
l Kut 3:6
Kut 6:3
m Mt 22:32
n Mt 22:42
Mk 12:35

43 mpaka niwaweke adui zako
kuwa kiti cha miguu yako."'[a]
44 Basi, Daudi anamwita 'Bwa-
na'; kwa hiyo inawezekanaje
kwamba yeye ni mwana wake?"

45 Ndipo, watu wote waki-
wa wanasikiliza akawaambia
wanafunzi:[b] 46 "Jihadhari-
ni na waandishi ambao huta-
mani kutembea wakiwa wa-
mevaa kanzu nao hupenda sa-
lamu katika masoko na viti
vya mbele katika masinago-
gi na mahali penye kuoneka-
na zaidi kwenye milo ya jioni,[c]
47 na ambao humeza nyumba
za wajane[d] na kutoa sala ndefu
kwa kisingizio. Hawa watapo-
kea hukumu nzito zaidi."[e]

21 Sasa alipotazama juu ali-
waona matajiri waki-
tumbukiza zawadi zao nda-
ni ya masanduku ya hazina.[f]
2 Ndipo akaona mjane fulani
mwenye uhitaji akitumbukiza
humo sarafu ndogo mbili za tha-
mani ndogo sana,[g] 3 naye
akasema: "Ninawaambia ninyi
kwa kweli, Mjane huyu, ijapo-
kuwa ni maskini, ametumbu-
kiza ndani zaidi kuliko hao
wote.[h] 4 Kwa maana wote
hawa walitumbukiza zawadi
kutokana na ziada yao, laki-
ni mwanamke huyu kutoka-
na na uhitaji wake alitumbuki-
za ndani riziki yote aliyokuwa
nayo."[i]

5 Baadaye, watu fulani wa-
lipokuwa wakisema kuhusu
hekalu, jinsi lilivyopambwa
kwa mawe mazuri na vitu vi-
livyowekwa wakfu,[j] 6 akase-
ma: "Vitu hivi ambavyo ninyi
mnaviona, siku zitakuja amba-
po hakuna jiwe litakaloachwa
hapa juu ya jiwe nalo lisiangu-
shwe chini."[a] 7 Ndipo waka-
muuliza, wakisema: "Mwali-
mu, kwa kweli mambo haya ya-
takuwa wakati gani, na ni nini
itakayokuwa ishara ya waka-
ti ambapo mambo hayo yatatu-
kia?"[b] 8 Akasema: "Jihadha-
rini msipotoshwe;[c] kwa maa-
na wengi watakuja kwa msingi
wa jina langu, wakisema,
'Mimi ndiye,' na, 'Wakati una-
ofaa umekaribia.'[d] Msiwafuate.
9 Zaidi ya hayo, wakati mna-
posikia juu ya vita na machafu-
ko, msiogope.[e] Kwa maana ma-
mbo hayo lazima yatukie kwa-
nza, lakini ule mwisho hauta-
tokea mara moja."

10 Ndipo akaendelea kuwa-
ambia: "Taifa litasimama ku-
pigana na taifa,[f] na ufalme
kupigana na ufalme;[g] 11 na
kutakuwa na matetemeko ma-
kubwa ya nchi, na katika ma-
hali pamoja baada ya pengi-
ne kutakuwa na tauni na
upungufu wa chakula;[h] kuta-
kuwa na mambo yenye kuogo-
pesha na ishara kubwa kutoka
mbinguni.[i]

12 "Lakini kabla ya mambo
yote hayo watu watawakamata
na kuwatesa,[j] wakiwakabidhi
ninyi kwenye masinagogi na
magereza, mkikokotwa na ku-
pelekwa mbele ya wafalme na
magavana kwa ajili ya jina la-
ngu.[k] 13 Utakuwa ushahidi
kwenu.[l] 14 Kwa hiyo azimie-
ni mioyoni mwenu kwamba
hamtafanya mazoezi mape-
ma ya jinsi mtakavyojitetea,[m]
15 kwa maana nitawapa ni-
nyi kinywa na hekima, amba-
yo wapinzani wenu wote waki-
wa pamoja hawataweza ku-
shindana nayo wala kubisha.[n]

SURA 20
a Zb 110:1
Mdo 2:34
b Mt 23:1
Mk 12:38
c Mt 23:6
Mk 12:39
d Isa 10:2
2Ti 3:6
e Mk 12:40

SURA 21
f Mk 12:41
g Mk 12:42
h Mk 12:43
2Ko 8:12
i Mt 22:37
Mk 12:44
j Mt 24:1
Mk 13:1

Safu ya 2
a 1Fa 9:7
1Fa 9:8
Yer 7:14
Mik 3:12
Mt 24:2
Mk 13:2
Lu 19:44
b Mt 24:3
Mk 13:4
c Efe 5:6
2Th 2:3
2Ti 3:13
1Yo 4:1
Ufu 12:9
d Mt 24:5
Mk 13:6
e Met 3:25
Mt 24:6
Mk 13:7
f Ufu 6:4
g Mt 24:7
Mk 13:8
h Mdo 11:28
Ufu 6:8
i Ufu 6:12
j Mt 10:17
Mk 13:9
Yoh 16:2
k Mt 24:9
Mk 13:9
Mdo 25:23
Ufu 2:10
l Flp 1:28
m Lu 12:11
n Mk 13:11
Mdo 6:10

16 Zaidi ya hayo, mtatolewa
hata na wazazi[a] na ndugu na ja-
maa zenu na rafiki zenu, nao
watafanya wengine kati yenu
wauawe;[b] **17** nanyi mtachu-
kiwa na watu wote kwa saba-
bu ya jina langu.[c] **18** Na bado
hata unywele[d] mmoja wa vi-
chwa vyenu hautaangamia.
19 Nanyi kwa kuvumilia mta-
jipatia nafsi zenu.[e]

20 "Zaidi ya hayo, mtakapo-
ona Yerusalemu limezingirwa[f]
na majeshi yaliyopiga kambi,
ndipo jueni kwamba kufanywa
ukiwa kwake kumekaribia.[g]
21 Ndipo wale walio katika Yu-
dea waanze kukimbilia milima-
ni, na wale walio katikati yake
na waondoke, nao wale walio
katika sehemu za mashambani
wasiingie ndani;[h] **22** kwa sa-
babu hizi ni siku za kupatili-
za haki, ili mambo yote yaliyo-
andikwa yatimizwe.[i] **23** Ole
wao wanawake wenye mimba
na wale wanaonyonyesha mto-
to mchanga katika siku hizo![j]
Kwa maana kutakuwa na uhi-
taji mkubwa juu ya nchi na
ghadhabu juu ya watu hawa;
24 nao wataanguka kwa ma-
kali ya upanga na watapele-
kwa mateka katika mataifa
yote;[k] na Yerusalemu litaka-
nyagwa-kanyagwa na mataifa,
mpaka nyakati zilizowekwa[l] za
mataifa zitimie.

25 "Pia, kutakuwa na ishara
katika jua[m] na mwezi na nyo-
ta, na juu ya dunia maumivu
makali ya mataifa, bila kujua
njia ya kutokea kwa sababu
ya kunguruma kwa bahari[n] na
msukosuko[o] wake, **26** huku
watu wakizimia kwa woga[p]
na tarajio la mambo yanayo-
kuja juu ya dunia inayokaliwa;[a]
kwa maana nguvu za mbingu zitatikiswa.[b] **27** Na ndipo watakapomwona Mwana wa binadamu[c] akija katika wingu akiwa na nguvu na utukufu mwingi.[d] **28** Lakini mambo haya yanapoanza kutukia, simameni wima na kuinua vichwa vyenu, kwa sababu ukombozi wenu unakaribia."

29 Ndipo akawaambia mfano: "Angalieni mtini na miti mingine yote:[e] **30** Wakati inapokuwa tayari imechipuka, kwa kuangalia mnajua wenyewe kwamba sasa kiangazi kiko karibu.[f] **31** Vivyo hivyo ninyi pia, wakati mnapoona mambo hayo yakitukia, jueni kwamba ufalme wa Mungu uko karibu.[g] **32** Kwa kweli nawaambia ninyi, Kizazi hiki hakitapitilia mbali kamwe mpaka mambo yote yatukie.[h] **33** Mbingu na dunia zitapitilia mbali,[i] lakini maneno yangu hayatapitilia mbali kamwe.[j]

34 "Lakini jiangalieni ninyi wenyewe kwamba mioyo yenu isilemewe kamwe na kula kupita kiasi na kunywa sana[k] na mahangaiko[l] ya maisha, na kwa ghafula siku hiyo iwe juu yenu mara moja[m] **35** kama mtego.[n] Kwa maana itakuja juu ya wale wote wanaokaa juu ya uso wa dunia yote.[o] **36** Basi, endeleeni kukesha[p] wakati wote mkiomba dua[q] ili mpate kufanikiwa kuponyoka mambo yote hayo yaliyokusudiwa kutukia, na kusimama mbele ya Mwana wa binadamu."[r]

37 Kwa hiyo wakati wa mchana alikuwa akifundisha

SURA 21

a 2Ti 3:3
b Mik 7:6
Mt 24:10
Mk 13:12
Mdo 7:59
c Mt 10:22
Mk 13:13
d 1Sa 14:45
Mt 10:30
Lu 12:7
e 2Nya 15:7
Ro 5:3
Ebr 10:36
2Pe 1:6
f Lu 19:43
g Da 9:26
Mt 23:38
Mt 24:15
h Mt 24:16
Mk 13:14
i Kum 32:35
Kum 32:43
Yer 5:29
Ho 9:7
j Mt 24:19
Mk 13:17
Lu 19:44
Lu 23:28
k Kum 28:64
Zb 79:1
Isa 63:18
Da 9:27
Zek 12:3
l Eze 21:26
Eze 21:27
Da 4:25
m Ufu 6:12
n Isa 57:20
Ufu 17:15
o Mt 24:29
Mk 13:24
p Sef 1:17

Safu ya 2

a Yoe 2:10
Yoe 2:30
b Isa 34:4
2Pe 3:10
c Da 7:13
d Mt 24:30
Mk 13:26
Ufu 1:7
e Mt 24:32
Mk 13:28
f Mt 24:33
g Mk 13:29
h Mt 24:34
Mk 13:30
i Mt 5:18
j Mt 24:35
Mk 13:31
Ufu 3:14
k Isa 5:11
l Mt 6:25
1Ti 6:8
m Met 11:4
Isa 5:13
Ro 13:13
n 1Th 5:3
o 1Th 5:2
2Pe 3:10
p Mt 25:13
Mk 13:33
q Ro 12:12
Efe 6:18
1Pe 4:7
r Mt 24:42
Mk 13:35
1Ko 16:13
1Pe 5:8
Ufu 6:17
Ufu 16:15

katika hekalu,[a] lakini wakati
wa usiku alikuwa akitoka kwe-
nda na kukaa juu ya mlima
unaoitwa Mlima wa Mizeituni.[b]
38 Na watu wote[c] walikuwa wa-
kimjia asubuhi katika hekalu ili
wamsikie.

22 Sasa sherehe ya keki
zisizo na chachu, ile
ambayo huitwa Pasaka,[d] iliku-
wa ikikaribia. **2** Pia, wakuu
wa makuhani na waandishi
walikuwa wakitafuta njia bora
ya kumwondolea mbali,[e] kwa
maana walikuwa wakiwaogo-
pa watu.[f] **3** Lakini Shetani
akamwingia Yuda, anayeitwa
Iskariote, ambaye alihesabi-
wa kati ya wale kumi na wa-
wili;[g] **4** naye akaenda zake
akaongea na wakuu wa maku-
hani na makapteni wa heka-
lu juu ya njia bora ya kumsa-
liti kwao.[h] **5** Basi, wakasha-
ngilia na kupatana kumpa fe-
dha.[i] **6** Kwa hiyo akakubali,
naye akaanza kutafuta nafa-
si nzuri ya kumsaliti kwao bila
umati kuwa karibu.[j]

7 Siku ya keki zisizo na cha-
chu sasa ikafika, ambapo mnya-
ma wa pasaka lazima atole-
we dhabihu;[k] **8** naye akawa-
tuma Petro na Yohana, akise-
ma: "Nendeni mkatutayarishie
pasaka[l] ili tule." **9** Wakamwa-
mbia: "Ni wapi unapotaka tuita-
yarishe?" **10** Akawaambia:[m]
"Tazameni! Mnapoingia katika
jiji, mwanamume anayebeba
chombo cha udongo cha maji
atakutana nanyi. Mfuateni
mwingie katika nyumba amba-
yo ataingia.[n] **11** Nanyi lazi-
ma mmwambie mwenye nyu-
mba hiyo, 'Mwalimu anakua-
mbia wewe: "Kiko wapi chumba
cha wageni ambacho humo ni-
naweza kula pasaka pamoja na
wanafunzi wangu?"'[a] **12** Na
mtu huyo atawaonyesha ninyi
chumba kikubwa cha juu che-
nye vifaa. Fanyeni matayarisho
humo."[b] **13** Kwa hiyo wakao-
ndoka na kukipata kama vile
alivyokuwa amewaambia, nao
wakatayarisha pasaka.[c]

14 Mwishowe saa ilipofika,
akaketi mezani, na wale mi-
tume pamoja naye.[d] **15** Naye
akawaambia: "Nimetamani
sana kula pasaka hii pamoja na-
nyi kabla sijateswa; **16** kwa
maana ninawaambia ninyi, Si-
taila tena mpaka itakapokuwa
imetimizwa katika ufalme wa
Mungu."[e] **17** Na, akipokea ki-
kombe,[f] akashukuru na kuse-
ma: "Chukueni hiki mkipitishe
kutoka kwa mmoja mpaka kwa
mwingine kati yenu; **18** kwa
maana ninawaambia ninyi, Ku-
toka sasa na kuendelea sita-
kunywa tena divai ya mzabibu
mpaka ufalme wa Mungu uta-
kapofika."[g]

19 Pia, akachukua mkate,[h]
akashukuru, akaumega, aka-
wapa, akisema: "Huu unamaa-
nisha mwili[i] wangu ambao uta-
tolewa kwa ajili yenu.[j] Ende-
leeni kufanya hivi kwa ku-
nikumbuka mimi."[k] **20** Pia,
kikombe[l] vivyo hivyo baada ya
wao kula mlo wa jioni, akase-
ma: "Kikombe hiki kinamaani-
sha agano[m] jipya kwa msingi
wa damu[n] yangu, ambayo ita-
mwagwa kwa ajili yenu.[o]

21 "Lakini, tazameni! mko-
no wa msaliti[p] wangu upo pa-
moja nami mezani.[q] **22** Kwa
sababu Mwana wa binadamu

SURA 21
a Lu 19:47
b Yoh 8:1
c Mk 12:37
Lu 19:48

SURA 22
d Kut 12:3
Law 23:5
Yoh 13:1
1Ko 5:7
e Lu 9:22
f Mt 21:46
Mt 26:4
Mk 14:2
Lu 20:19
g Mt 26:14
Mk 14:10
Yoh 6:70
Yoh 13:2
Yoh 13:27
Mdo 1:17
h Yoh 13:18
i Zek 11:12
Mt 26:15
1Ti 6:10
Yud 11
j Mt 26:16
Mk 14:11
k Kut 12:14
Kut 12:18
Law 23:6
Kum 16:2
Mt 26:17
Mk 14:12
l Kut 12:8
m 1Sa 10:3
n Mt 26:18
Mk 14:13

Safu ya 2
a Mk 14:14
b Mk 14:15
c Mt 26:19
Mk 14:16
Lu 19:32
d Mt 26:20
Mk 14:17
e Lu 13:29
Lu 14:15
f 1Ko 10:16
1Ko 11:25
g Ufu 19:9
h Kut 12:8
Kut 12:20
Kum 16:3
1Ko 10:17
1Ko 11:23
i Yoh 6:51
1Ko 10:16
j Ebr 10:10
1Pe 2:24
k Mt 26:26
Mk 14:22
1Ko 11:24
l Mk 14:23
1Ko 10:16
m Yer 31:31
Yer 32:40
2Ko 3:6
Ebr 7:22
Ebr 8:8
n Kut 24:8
Zek 9:11
Mt 26:28
1Ko 11:25
Ebr 9:18
o Zb 50:5
Mt 26:28
Mk 14:24
Ebr 2:16
Ebr 9:14
1Pe 1:19
p Zb 41:9
q Mt 26:21; Yoh 13:21.

anaenda zake kulingana na ili-
vyopangwa;[a] hata hivyo, ole
wake mtu yule ambaye kupi-
tia kwake huyo atasalitiwa!"[b]
23 Kwa hiyo wakaanza kuu-
lizana ni nani kati yao amba-
ye kwa kweli ndiye angefanya
hivyo.[c]

24 Hata hivyo, kukatokea
pia bishano kali kati yao juu
ya ni nani kati yao aliyeoneka-
na kuwa mkuu zaidi ya wote.[d]
25 Lakini akawaambia: "Wafa-
lme wa mataifa hupiga ubwana
juu yao, na wale walio na ma-
mlaka juu yao huitwa Wafadhi-
li.[e] **26** Ingawa hivyo, ninyi
hampaswi kuwa hivyo.[f] Lakini
acheni yule aliye mkuu zaidi ya
wote kati yenu awe kama aliye
mdogo zaidi ya wote,[g] na yule
anayetenda kama mkuu kama
yule anayehudumu.[h] **27** Kwa
maana ni nani aliye mkuu za-
idi, yule anayeketi mezani au
yule anayehudumu? Je, si
yule anayeketi mezani? Lakini
mimi nimo katikati yenu kama
yule anayehudumu.[i]

28 "Hata hivyo, ninyi ndio
mmeshikamana[j] nami katika
majaribu yangu;[k] **29** nami
ninafanya agano pamoja na-
nyi, sawa na vile Baba ya-
ngu alivyofanya agano[l] pamo-
ja nami, kwa ajili ya ufa-
lme,[m] **30** ili mpate kula[n] na
kunywa mezani pangu katika
ufalme wangu,[o] na kuketi juu
ya viti vya ufalme[p] kuyahuku-
mu makabila kumi na mawili
ya Israeli.

31 "Simoni, Simoni, tazama!
Shetani[q] amedai kuwapata ni-
nyi ili awapepete kama ngano.[r]
32 Lakini nimeomba dua[s] kwa
ajili yako ili imani yako isifi-
fie; na wewe, mara tu utaka-
pokuwa umerudi, watie ngu-
vu[a] ndugu zako." **33** Ndipo
akamwambia: "Bwana, mimi
niko tayari kwenda pamoja
nawe gerezani na pia katika
kifo."[b] **34** Lakini akasema:
"Ninakuambia wewe, Petro,
Jogoo hatawika leo mpaka uwe
umekana mara tatu kuwa hu-
nijui."[c]

35 Akawaambia wao pia:
"Wakati nilipowatuma[d] ninyi
bila mkoba na mfuko wa cha-
kula na viatu, je, mlikosa kitu
chochote?" Wakasema: "Hapa-
na!" **36** Ndipo akawaambia:
"Lakini sasa acheni yule amba-
ye ana mkoba auchukue, vi-
vyo hivyo pia mfuko wa cha-
kula; na acheni yule asiye na
upanga auze vazi lake la nje
na kununua mmoja. **37** Kwa
maana nawaambia ninyi kwa-
mba lazima hili ambalo lime-
andikwa litimizwe kwangu,
yaani, 'Naye alihesabiwa pa-
moja na waasi-sheria.'[e] Kwa
maana kile kinachonihusu ki-
natimia."[f] **38** Ndipo waka-
sema: "Bwana, tazama! hapa
pana panga mbili." Akawaa-
mbia: "Inatosha."

39 Alipotoka nje kama ili-
vyo desturi alienda kwenye Mli-
ma wa Mizeituni; na wanafu-
nzi pia wakamfuata.[g] **40** Baa-
da ya kufika hapo akawaambia:
"Salini, ili msiingie katika ja-
ribu."[h] **41** Naye mwenyewe
akaondoka kwao karibu umba-
li wa mtupo wa jiwe, akapi-
ga magoti na kuanza kusali,
42 akisema: "Baba, ikiwa una-
taka, niondolee kikombe hiki.
Hata hivyo, acha, si mapenzi
yangu,[i] bali yako yatendeke."[j]

SURA 22

a Isa 53:1-12
Da 9:26
Mdo 4:28
1Pe 1:11
b Mt 26:24
c Mt 26:22
Mk 14:19
Yoh 13:22
d Mk 9:34
Lu 9:46
e Mt 20:25
Mk 10:42
f 1Pe 5:3
g Lu 9:48
h Mt 20:26
Mk 10:43
Lu 9:48
i Mt 20:28
Yoh 13:4
Flp 2:7
j Yoh 6:67
k Ro 8:17
Ebr 4:15
l Zb 110:4
m Da 7:27
Lu 12:32
2Ti 2:12
Ebr 12:28
Yak 2:5
Ufu 1:6
n Lu 12:37
Ufu 19:9
o Lu 13:29
Yoh 17:24
p Mt 19:28
1Ko 6:2
Ufu 2:26
Ufu 3:21
Ufu 20:6
q 2Ko 2:11
1Pe 5:8
r Amo 9:9
Mt 26:31
Mk 14:27
s Yoh 17:15
Ebr 7:25
1Yo 2:1

Safu ya 2

a Isa 35:3
b Mt 26:33
Mk 14:29
Yoh 13:37
c Mt 26:34
Mk 14:30
Lu 22:61
Yoh 13:38
d Mt 10:9
Mk 6:8
Lu 9:3
e Isa 53:12
f Lu 18:31
g Mt 26:30
Mk 14:26
Yoh 18:1
h Mt 26:41
Mk 14:38
Lu 22:46
i Mt 26:39
Mk 14:39
j Mt 6:10
Mk 14:36
Yoh 5:30
Yoh 6:38

43 Ndipo malaika kutoka mbinguni akamtokea akamtia
nguvu.[a] **44** Lakini akaingia
katika maumivu makali, akaendelea kusali kwa bidii zaidi;[b]
na jasho lake likawa kama ma-
tone ya damu yakianguka chini.[c] **45** Naye akaondoka baa-
da ya sala, akawaendea wa-
nafunzi, akawakuta wakisi-
nzia kwa huzuni;[d] **46** naye
akawaambia: "Kwa nini mna-
lala usingizi? Amkeni msali, ili
msiingie katika jaribu."[e]

47 Alipokuwa bado akise-
ma, tazama! umati, na yule
mtu anayeitwa Yuda, mmo-
ja wa wale kumi na wawili,
alikuwa akienda mbele yao;[f]
naye akamkaribia Yesu ili ku-
mbusu.[g] **48** Lakini Yesu aka-
mwambia: "Yuda, je, wewe
unamsaliti Mwana wa binada-
mu kwa busu?"[h] **49** Wale wa-
liokuwa kandokando yake wa-
lipoona jambo lililokuwa kari-
bu kutukia, wakasema: "Bwa-
na, je, tupige kwa upanga?"[i]
50 Mtu fulani kati yao hata
alimpiga mtumwa wa kuhani
mkuu, akalikata sikio lake la
kuume.[j] **51** Lakini Yesu aka-
jibu, akasema: "Basi, acheni,
inatosha." Naye akagusa si-
kio na kumponya.[k] **52** Ndi-
po Yesu akawaambia wakuu
wa makuhani na makapteni
wa hekalu na wanaume wazee
waliokuwa wamekuja hapo
kumchukua: "Je, mlitoka mki-
wa na mapanga na marungu
kana kwamba ni juu ya mnya-
ng'anyi?[l] **53** Nilipokuwa pa-
moja nanyi katika hekalu[m]
siku baada ya siku hamkunyo-
osha mikono yenu ili kunika-
mata.[n] Lakini hii ndiyo saa[o]
yenu na ndiyo mamlaka[a] ya
giza."[b]

54 Ndipo wakamkamata,
wakampeleka[c] na kumwingi-
za katika nyumba ya kuhani
mkuu;[d] lakini Petro alikuwa
akifuata kwa umbali fulani.[e]
55 Walipowasha moto katikati
ya ua na kuketi chini pamoja,
Petro alikuwa ameketi katika-
ti yao.[f] **56** Lakini kijakazi fu-
lani akamwona ameketi kando
ya ule moto mwangavu aka-
mtazama kwa kumchunguza
na kusema: "Mtu huyu pia ali-
kuwa pamoja naye."[g] **57** La-
kini akakana,[h] akisema: "Wee
mwanamke, mimi simjui."[i]
58 Na baada ya muda mfupi
mtu mwingine akamwona
akasema: "Wewe pia ni mmo-
ja wao." Lakini Petro akasema:
"Wee mtu, si mimi."[j] **59** Na
baada ya karibu muda wa saa
moja kupita mtu mwingine
akaanza kusisitiza kwa nguvu:
"Kwa hakika mtu huyu pia ali-
kuwa pamoja naye; kwa maa-
na, kwa kweli, yeye ni Mgalila-
ya!"[k] **60** Lakini Petro akase-
ma: "Wee mtu, mimi sijui unalo-
sema." Na mara tu, alipokuwa
bado akisema, jogoo akawika.[l]
61 Na Bwana akageuka, aka-
mtazama Petro, na Petro aka-
kumbuka maneno ya Bwana
alipomwambia: "Kabla ya jogoo
kuwika leo utanikana mara
tatu."[m] **62** Naye akaenda nje
akalia kwa uchungu.[n]

63 Sasa wale wanaume wa-
liokuwa wakimlinda kifungoni
wakaanza kumdhihaki,[o] waki-
mpiga;[p] **64** na baada ya ku-
mfunika wakawa wakiuliza na
kusema: "Toa unabii. Ni nani
aliyekupiga?"[q] **65** Nao waka-

SURA 22

a 1Fa 19:5
Isa 49:8
Da 10:18
Mt 4:11
b Yoh 12:27
Ebr 5:7
c Isa 53:7
Isa 53:10
Lu 12:50
d Mt 26:40
Mk 14:37
e Mt 26:41
Mk 14:38
Lu 22:40
f Mt 26:47
Mk 14:43
Yoh 18:2
g 2Sa 20:9
h Mt 26:48
Mk 14:45
i Lu 22:36
j Mt 26:51
Mk 14:47
Yoh 18:10
k Yoh 18:11
l Mt 26:55
Mk 14:48
m Lu 19:47
n Yoh 7:30
o Yoh 12:27

Safu ya 2

a Yoh 19:11
b Kol 1:13
c Isa 53:7
Mdo 8:32
d Mt 26:57
e Mt 26:58
Mk 14:54
Yoh 18:15
f Yoh 18:18
g Mt 26:69
Mk 14:67
h Met 29:25
i Mt 26:70
Mk 14:68
j Mt 26:71
Mk 14:69
Yoh 18:25
k Mt 26:73
Mk 14:70
Yoh 18:26
l Mt 26:74
Mk 14:71
Yoh 18:27
m Mt 26:75
Mk 14:72
n Isa 66:2
Eze 7:16
1Ko 10:12
2Ko 7:10
o Zb 22:7
p Isa 50:6
Isa 53:5
Mt 26:67
Mk 14:65
q Mt 26:68

endelea kusema mambo me-
ngine mengi ya kumkufuru.[a]
66 Hatimaye kulipokuwa
mchana, kusanyiko la wanau-
me wazee wa watu, wakuu wa
makuhani na waandishi pia,
wakakusanyika pamoja,[b] nao
wakamkokota na kumwingiza
ndani ya jumba lao la Sanhe-
drini, wakisema:[c] **67** "Ikiwa
wewe ndiye Kristo,[d] tuam-
bie." Lakini akawaambia:
"Hata kama ningewaambia, ni-
nyi hamngeamini hata kido-
go.[e] **68** Zaidi ya hayo, kama
ningewauliza ninyi, hamngeji-
bu hata kidogo.[f] **69** Hata hi-
vyo, kutoka sasa na kuendelea
Mwana wa binadamu[g] ataku-
wa akiketi kwenye mkono wa
kuume[h] wenye nguvu wa Mu-
ngu."[i] **70** Ndipo wote waka-
sema: "Kwa hiyo, je, wewe ndi-
ye Mwana wa Mungu?" Akawa-
ambia: "Ninyi wenyewe mna-
sema[j] kwamba mimi ndiye."
71 Wakasema: "Kwa nini tu-
nahitaji ushahidi zaidi?[k] Kwa
maana sisi wenyewe tumelisi-
kia kutoka katika kinywa cha-
ke mwenyewe."[l]

23 Kwa hiyo umati huo
ukasimama, wote pamo-
ja, na kumpeleka kwa Pilato.[m]
2 Ndipo wakaanza kumshta-
ki,[n] wakisema: "Tulimkuta
mtu huyu akipindua[o] taifa letu
na kuwakataza watu wasimlip-
e Kaisari kodi[p] na kusema
kwamba yeye mwenyewe ni
Kristo mfalme."[q] **3** Sasa Pila-
to akamuuliza: "Je, wewe ndi-
ye mfalme wa Wayahudi?" Aka-
mjibu, akasema: "Wewe mwe-
nyewe unasema."[r] **4** Ndipo
Pilato akawaambia wakuu wa
makuhani na ule umati: "Mimi

SURA 22
a Zb 44:16
Isa 51:7
b Zb 2:2
Mdo 4:26
c Mt 27:1
Mk 15:1
d Mt 26:63
Mk 14:61
Yoh 10:24
e Yoh 3:12
Yoh 8:45
f Lu 20:7
g Da 7:13
Ufu 1:7
h Zb 110:1
i Mt 26:64
Mk 14:62
Mdo 2:33
Mdo 7:55
Ro 8:34
Kol 3:1
Ebr 1:3
j Mt 27:11
Mk 15:2
k Kum 17:6
l Mt 26:65
Mk 14:63

SURA 23
m Mt 27:2
Mk 15:1
Yoh 18:28
n 1Fa 21:10
Zb 35:11
o Yoh 12:19
Mdo 24:5
p Met 25:18
Mk 12:17
q Yoh 1:49
Yoh 18:36
r Mt 27:11
1Ti 6:13

Safu ya 2
a Yoh 18:38
Ebr 7:26
1Pe 2:22
b Lu 3:1
c Lu 9:9
d Mt 14:1
Mk 6:14
e Zb 39:1
Isa 53:7
f Mdo 25:7
g Isa 53:3
Lu 9:22
h Zb 22:7
i Mdo 4:27

sioni uhalifu wa mtu huyu."[a]
5 Lakini wao wakaanza kusi-
sitiza, wakisema: "Yeye huwa-
chochea watu kwa kufundisha
katika Yudea yote, hata kua-
nzia Galilaya mpaka hapa."
6 Aliposikia hilo, Pilato aka-
uliza kama mtu huyo aliku-
wa Mgalilaya, **7** na, baada ya
kuhakikisha kwamba alikuwa
wa kutoka eneo la utawala wa
Herode,[b] akampeleka kwa He-
rode, ambaye yeye mwenyewe
pia alikuwa katika Yerusalemu
siku hizo.
8 Herode alipomwona Yesu
alishangilia sana, kwa maa-
na kwa muda mrefu alikuwa
akitaka kumwona[c] kwa saba-
bu alikuwa amesikia[d] juu yake,
na alikuwa akitumaini kuo-
na ishara fulani kutoka kwa-
ke. **9** Sasa akaanza kumuu-
liza maswali kwa maneno me-
ngi sana; lakini yeye hakumji-
bu.[e] **10** Hata hivyo, wakuu
wa makuhani na waandishi
wakaendelea kusimama na ku-
mshtaki kwa ukali.[f] **11** Ndi-
po Herode pamoja na askari-
jeshi wake walinzi wakam-
fedhehesha,[g] naye akamdhi-
haki[h] kwa kumvika vazi
jangavu na kumrudisha kwa
Pilato. **12** Wote wawili Hero-
de na Pilato[i] sasa wakawa ma-
rafiki siku ileile; kwa maana
kabla ya hapo walikuwa na ua-
dui kati yao wenyewe.
13 Ndipo Pilato akawaita
pamoja wakuu wa makuha-
ni na watawala na watu **14** na
kuwaambia: "Mliniletea mtu
huyu kama mtu anayewacho-
chea watu waasi, na, tazame-
ni! mimi nilimhoji mbele
yenu lakini sikupata katika

mtu huyu msingi[a] wa mashtaka
mnayoleta juu yake. **15** Kwa
kweli, wala Herode hakupata,
kwa maana alimrudisha kwe-
tu; na, tazama! hajafanya lolo-
te linalostahili kifo.[b] **16** Kwa
hiyo nitamwadhibu[c] na kumfu-
ngua." **17** —— **18** Lakini
wakiwa pamoja na umati, wao
wote wakapaaza sauti, wakise-
ma: "Mwondolee mbali huyu,[d]
lakini tufungulie Baraba!"[e]
19 (Huyo ni mtu aliyekuwa
ametupwa gerezani kwa saba-
bu ya uchochezi wa uasi fulani
uliotukia katika jiji na kwa
kuua.) **20** Tena Pilato akawa-
paazia sauti, kwa sababu alita-
ka kumfungua Yesu.[f] **21** Ndi-
po wakaanza kupiga kelele,
wakisema: "Mtundike mtini!
Mtundike mtini!"[g] **22** Mara
ya tatu akawaambia: "Kwa
nini, ni jambo gani baya ali-
lofanya mtu huyu? Mimi sikuo-
na jambo lolote linalostahi-
li kifo ndani yake; kwa
hiyo nitamwadhibu na ku-
mfungua."[h] **23** Ndipo wakaa-
nza kufanya haraka-haraka,
kwa sauti zilizo kubwa, wa-
kidai kwamba atundikwe mti-
ni; na sauti zao zikaanza ku-
shinda.[i] **24** Kwa hiyo Pila-
to akatoa hukumu ili dai lao
litimizwe:[j] **25** akamfungua[k]
yule mtu aliyekuwa ametupwa
gerezani kwa uchochezi wa
uasi na kuua na ambaye wao
walikuwa wakidai, lakini aka-
mtia Yesu mikononi mwao wa-
mtendee wanavyopenda.[l]

26 Sasa walipokuwa wakim-
peleka, walimshika Simoni,
mzaliwa wa Kirene, akija ku-
toka mashambani, nao waka-
mtwika mti wa mateso aube-

SURA 23

a Yoh 18:38
b Mdo 23:29
c Mt 27:26
Yoh 19:1
d Isa 49:7
e Mt 27:20
Mk 15:11
Yoh 18:40
f Mt 27:22
Mk 15:12
Yoh 19:12
g Mk 15:13
Yoh 19:6
h Mt 27:23
Mk 15:14
i Kut 23:2
Yoh 19:15
j Mk 15:15
Yoh 19:16
k Met 17:15
l Mt 27:26

Safu ya 2

a Mk 15:21
Yoh 19:17
b Kum 28:57
Yer 9:19
Mk 13:17
Lu 19:44
c Mt 24:19
Lu 21:23
d Isa 2:19
Ho 10:8
Ufu 6:16
e Met 11:31
Yer 25:29
Eze 20:47
1Pe 4:17
f Isa 53:12
Mt 27:38
g Mt 27:33
h Yoh 19:18
i Mdo 7:60
j Zb 22:18
Isa 53:12
Mt 27:35
Mk 15:24
k Zek 12:10
l Zb 22:8

be nyuma ya Yesu.[a] **27** La-
kini kulikuwa na umati mku-
bwa wa watu na wa wanawake
ambao walimfuata waliokuwa
wakijipiga-piga kwa huzuni na
kumwombolezea. **28** Yesu
akawageukia wanawake hao
na kusema: "Binti za Yerusa-
lemu, acheni kunililia. Bada-
la yake, jililieni ninyi wenye-
we na watoto wenu;[b] **29** kwa
sababu, tazameni! siku zina-
kuja ambapo watu watasema,
'Wenye furaha ni wanawake
walio tasa, na matumbo ya
uzazi ambayo hayakuzaa na
maziwa ambayo hayakunyo-
nyesha!'[c] **30** Ndipo wataka-
poanza kuiambia milima, 'Tu-
angukieni!' na vilima, 'Tufuni-
keni!'[d] **31** Kwa sababu ikiwa
wao wanafanya mambo haya
wakati mti ni mbichi, itakuwa-
je utakapokuwa umekauka?"[e]

32 Lakini watu wengine wa-
wili, watenda-maovu, wali-
kuwa pia wakipelekwa waka-
uawe pamoja naye.[f] **33** Nao
walipofika mahali panapoi-
twa Fuvu la Kichwa,[g] huko
wakamtundika mtini yeye na
wale watenda-maovu, mmo-
ja upande wake wa kuume na
mwingine upande wake wa ku-
shoto.[h] **34** [[Lakini Yesu ali-
kuwa akisema: "Baba, wasa-
mehe,[i] kwa maana hawajui wa-
nalofanya."]] Zaidi ya hayo, ili
kugawa mavazi yake, waka-
piga kura.[j] **35** Na wale watu
wakasimama wakitazama.[k]
Lakini wale watawala wali-
kuwa wakicheka kwa dharau,
wakisema:[l] "Aliwaokoa wengi-
ne; mwacheni ajiokoe mwenye-
we, ikiwa huyu ndiye Kristo
wa Mungu, Yule Aliyechaguli-

wa."[a] **36** Hata wale askari
wakamdhihaki,[b] wakija karibu
na kumpa divai kali[c] **37** na
kusema: "Ikiwa wewe ndiye
mfalme wa Wayahudi, jiokoe
mwenyewe." **38** Kulikuwa
pia na maandishi juu yake:
"Huyu ndiye mfalme wa Waya-
hudi."[d]

39 Lakini mmoja wa wale
watenda-maovu waliotundi-
kwa akaanza kumwambia kwa
maneno ya matusi: "Wewe ndi-
ye Kristo, sivyo? Jiokoe mwe-
nyewe na sisi." **40** Yule mwi-
ngine akamjibu, akamkemea
na kusema: "Je, wewe humwo-
gopi Mungu hata kidogo, kwa
kuwa sasa umo katika hukumu
ileile?[f] **41** Nasi, kwa kweli,
tuko hivyo kwa haki, kwa ma-
ana sisi tunapokea kwa ukami-
li kile tunachostahili kwa ma-
mbo tuliyofanya; lakini mtu
huyu hakufanya jambo lolote
lisilofaa."[g] **42** Naye aka-
endelea kusema: "Yesu, uni-
kumbuke utakapoingia katika
ufalme wako."[h] **43** Naye aka-
mwambia: "Kwa kweli mimi
nakuambia leo, Utakuwa pa-
moja nami[i] katika Paradiso."[j]

44 Basi, kufikia sasa ilikuwa
karibu saa sita, na hata hivyo
kukawa na giza juu ya dunia
yote mpaka saa tisa,[k] **45** kwa
sababu nuru ya jua ilikosekana;
ndipo pazia[l] la patakatifu lika-
pasuka katikati.[m] **46** Na Yesu
akaita kwa sauti kubwa na ku-
sema: "Baba, ninaikabidhi roho
yangu mikononi mwako."[n] Ali-
pokuwa amesema jambo hilo,
akakata pumzi.[o] **47** Kwa sa-
babu ya kuona lililokuwa lime-
tukia yule ofisa-jeshi akaanza
kumtukuza Mungu, akisema:
"Kwa kweli mtu huyu aliku-
wa mwadilifu."[a] **48** Na uma-
ti wote uliokuwa umekusanyi-
ka pamoja hapo kwa ajili ya
tukio hilo, walipoyaona ma-
mbo yaliyotukia, wakaanza ku-
rudi, wakipiga-piga vifua vyao.
49 Zaidi ya hayo, wale wote
waliojuana naye walikuwa wa-
mesimama umbali fulani.[b] Pia,
wanawake, waliokuwa wame-
mfuata pamoja kutoka Galila-
ya, walikuwa wamesimama wa-
kiona mambo haya.[c]

50 Na, tazama! mwanamu-
me aliyeitwa Yosefu, ambaye
alikuwa mshiriki wa Baraza,
mtu mwema na mwadilifu[d]—
51 mtu huyu hakuwa amepi-
ga kura katika kuunga mkono
mbinu yao na tendo[e]—aliku-
wa wa kutoka Arimathea, jiji
moja la Wayudea, naye aliku-
wa akiungojea ufalme wa Mu-
ngu;[f] **52** mtu huyu alimwe-
ndea Pilato na kuomba apewe
mwili wa Yesu.[g] **53** Naye aka-
ushusha[h] na kuufunga katika
kitani bora, naye akamlaza ka-
tika kaburi[i] lililochongwa kati-
ka mwamba, ambamo haku-
na mtu aliyepata kulazwa.[j]
54 Sasa ilikuwa ni siku ya Ma-
tayarisho,[k] na nuru ya jioni
ya siku ya sabato[l] ilikuwa iki-
karibia. **55** Lakini wale wa-
nawake, waliokuwa wamekuja
pamoja naye kutoka Galilaya,
wakafuata, wakalitazama ka-
buri[m] na jinsi mwili wake uli-
vyolazwa;[n] **56** nao wakarudi
kutayarisha manukato na ma-
futa yaliyotiwa marashi.[o] Laki-
ni, bila shaka, walipumzika
siku ya sabato[p] kulingana na
amri.

SURA 23
a Mt 27:42
Mk 15:31
b Zb 22:7
c Zb 69:21
d Mt 27:37
Mk 15:26
Yoh 19:19
e Mt 26:68
Mt 27:44
Mk 15:32
f Yer 5:3
g 1Pe 1:19
h Lu 1:32
i Yoh 5:29
Mdo 24:15
j Isa 11:6
Isa 35:1
Isa 65:17
Ufu 21:1
k Amo 8:9
Mt 27:45
Mk 15:33
l Kut 26:31
Kut 36:35
m Ebr 10:20
n Zb 31:5
Mdo 7:59
o Mt 27:50

Safu ya 2
a Mt 27:54
b Zb 38:11
Zb 88:8
c Mt 27:55
Mk 15:40
Lu 8:2
d Mt 27:57
Mk 15:43
Yoh 19:38
e Mwa 37:21
f Mk 15:43
Lu 2:25
g Mt 27:58
h Kum 21:23
i Isa 53:9
j Mt 27:59
Mk 15:46
k Kut 12:6
Mt 27:62
Mk 15:42
Yoh 19:42
l Kut 20:10
Kum 5:14
m Yoh 5:28
n Mt 27:61
Mk 15:47
o Mt 26:7
p Kut 16:29
Kut 20:8
Kut 31:15
Kum 5:12

24 Hata hivyo, siku ya
kwanza ya juma walie-
nda mapema sana kwenye ka-
buri, wakichukua yale manu-
kato waliyokuwa wametaya-
risha.[a] **2** Lakini wakapata
jiwe limeviringishwa kutoka
kwenye kaburi,[b] **3** nao wali-
poingia hawakuupata mwi-
li wa Bwana Yesu.[c] **4** Wali-
pokuwa wakifadhaika juu ya
hilo, tazama! wanaume wa-
wili waliovaa mavazi yenye
kung'aa wakasimama kando
yao.[d] **5** Kwa kuwa hao wana-
wake waliogopa sana na kui-
namisha nyuso zao chini,
wale wanaume wakawaambia:
"Kwa nini mnatafuta yule Ali-
ye hai kati ya wafu? **6** [[Ha-
yupo hapa, bali amefufuliwa.]][e]
Kumbukeni jinsi alivyowaa-
mbia alipokuwa angali kati-
ka Galilaya,[f] **7** akisema kwa-
mba Mwana wa binadamu la-
zima atiwe mikononi mwa
watu wenye dhambi na ku-
tundikwa mtini na bado siku
ya tatu afufuliwe."[g] **8** Kwa
hiyo wakakumbuka[h] maneno
yake, **9** nao wakarudi kuto-
ka kwenye kaburi wakawapa
habari ya mambo hayo yote
wale kumi na mmoja na wale
wengine wote.[i] **10** Walikuwa Magdalene Maria, na Yoa-
na,[j] na Maria mama ya Yako-
bo. Pia, wengine kati ya wana-
wake[k] waliokuwa pamoja nao
walikuwa wakiwaeleza mitu-
me mambo hayo. **11** Hata hi-
yo, maneno hayo yalioneka-
na kama upuuzi kwao nao wa-
kawa hawawaamini[l] wanawa-
ke hao.

12 [[Lakini Petro akaondo-
ka, akakimbia kwenda kwenye
kaburi, akainama mbele, aka-
ona vile vitambaa peke yake.
Kwa hiyo akaenda zake, aki-
staajabu ndani yake mwenye-
we juu ya lililokuwa limetu-
kia.]]

13 Lakini, tazama! siku ile-
ile wawili kati yao walikuwa
safarini kwenda kijiji kilicho
umbali wa karibu kilometa
kumi na moja kutoka Yerusa-
lemu na kinachoitwa Emau,
14 nao walikuwa wakiongea
pamoja juu ya mambo yote
haya[a] yaliyokuwa yametukia.

15 Sasa walipokuwa wakio-
ngea na kujadiliana, Yesu aka-
karibia,[b] akaanza kutembea
pamoja nao; **16** lakini macho
yao yalizuiwa wasiweze kumta-
mbua.[c] **17** Akawaambia: "Ni
mambo gani haya ambayo mna-
jadiliana kati yenu wenyewe
mnapotembea?" Nao wakasi-
mama tuli wakiwa na nyuso
zenye huzuni. **18** Yule aliye-
itwa Kleopa akajibu, akamwa-
mbia: "Je, wewe unakaa peke
yako kama mgeni katika Ye-
rusalemu na kwa hiyo huya-
jui mambo ambayo yametu-
kia humo siku hizi?" **19** Naye
akawaambia: "Mambo gani?"
Wakamwambia: "Yale mambo
kuhusu Yesu Mnazareti,[d] ali-
yekuwa nabii[e] mwenye ngu-
vu katika kazi na neno mbe-
le za Mungu na watu wote;
20 na jinsi wakuu wa maku-
hani wetu na watawala wali-
yomkabidhi kwenye hukumu
ya kifo na kumtundika mtini.[f]
21 Lakini sisi tulikuwa tuki-
tumaini kwamba mtu huyu
ndiye angekomboa Israeli;[g] ndi-
yo, na mbali na mambo yote
haya, hii ndiyo siku ya tatu

SURA 24

a Mt 28:1
Mk 16:1
Yoh 20:1

b Mk 16:4

c Mk 16:5

d Amu 13:6
Mt 28:5
Mdo 1:10

e Mt 28:6
Mk 16:6

f Mt 28:7
Mk 16:7

g Yon 1:17
Mt 16:21
Mk 8:31
Lu 9:22
Mdo 17:3

h Yoh 2:22

i Mt 28:8

j Lu 8:3

k Lu 8:2

l Mwa 45:26

Safu ya 2

a Lu 9:22

b Mt 18:20

c Yoh 20:14
Yoh 21:4

d Mt 2:23
Mt 21:11

e Kum 18:18
Lu 7:16
Yoh 3:2
Yoh 6:14
Mdo 2:22

f Lu 23:1
Mdo 3:13
Mdo 13:27

g Mdo 1:6

tangu mambo hayo yalipotukia. **22** Zaidi ya hayo, wanawake[a] fulani kutoka kati yetu walitushangaza pia, kwa sababu walikuwa wamefika mapema kwenye kaburi **23** lakini hawakuupata mwili wake nao wakaja wakisema walikuwa pia wameona maono ya malaika yanayozidi nguvu za asili, waliosema kwamba yeye yuko hai. **24** Na zaidi, baadhi ya hao walio pamoja nasi walienda kwenye kaburi;[b] nao wakalikuta hivyo, kama vile wale wanawake walivyokuwa wamesema, lakini hawakumwona."

25 Kwa hiyo akawaambia: "Enyi wasio na akili na wazito katika moyo kuyaamini mambo yote waliyosema manabii![c] **26** Je, haikuwa lazima Kristo kupatwa[d] na mambo haya na kuingia katika utukufu wake?"[e] **27** Naye akaanzia Musa[f] na Manabii[g] wote, akawafasiria mambo yanayomhusu yeye mwenyewe katika Maandiko yote.

28 Mwishowe wakaja karibu na kijiji walikokuwa wakienda, naye akajifanya kana kwamba alikuwa akisafiri kwenda mbali zaidi. **29** Lakini wakamkaza, wakisema: "Kaa pamoja nasi, kwa sababu jioni imekaribia na mchana tayari umekwisha." Ndipo akaingia akae pamoja nao. **30** Naye alipokuwa ameketi pamoja nao kwenye mlo akauchukua mkate, akaubariki, akaumega na kuanza kuwapa.[h] **31** Ndipo macho yao yakafunguliwa kikamili nao wakamtambua; naye akatoweka kutoka kwao.[i]

SURA 24

a Mt 28:8
Lu 24:10

b Lu 24:12
Yoh 20:3

c Zb 22:Uta-31
Isa 53:1-12
Yoh 20:27

d Mdo 17:3
1Ko 15:3

e Yoh 20:9
Flp 2:9
Ebr 2:9
1Pe 1:11

f Mwa 3:15
Mwa 22:18
Mwa 49:10
Hes 21:9
Kum 18:15

g Isa 7:14
Isa 9:6
Yer 23:5
Eze 34:23
Da 9:24
Mik 5:2
Mal 3:1
Yoh 1:45
Mdo 10:43
Mdo 26:22

h Mt 14:19
Mt 15:36
Mk 6:41

i Yoh 20:19

Safu ya 2

a 1Ko 15:5

b Lu 9:16

c Mt 14:26

d 1Yo 1:1

e 1Ko 15:50

f Mwa 45:26

g Yoh 21:5

h Yoh 21:13

i Mdo 10:41

32 Nao wakaambiana: "Je, mioyo yetu haikuwa ikiwaka alipokuwa akisema nasi barabarani, alipokuwa akitufungulia Maandiko?" **33** Na saa ileile wakaondoka, wakarudi Yerusalemu, nao wakawakuta wale kumi na mmoja na wale walio pamoja nao wamekusanyika pamoja, **34** wakisema: "Kwa kweli Bwana alifufuliwa naye alimtokea Simoni!"[a] **35** Sasa wao wenyewe wakasimulia yale matukio barabarani na jinsi walivyopata kumjua kwa kule kuumega mkate.[b]

36 Walipokuwa wakisema juu ya mambo hayo yeye mwenyewe akasimama katikati yao [[na kuwaambia: "Na muwe na amani."]] **37** Lakini kwa sababu wao walikuwa wameogopa,[c] na walikuwa na hofu sana, walikuwa wakiwazia wameona roho. **38** Kwa hiyo akawaambia: "Kwa nini mnafadhaika, na kwa nini shaka zinatokea mioyoni mwenu? **39** Oneni mikono na miguu yangu, kwamba ni mimi mwenyewe; niguseni[d] mwone, kwa sababu roho haina nyama na mifupa[e] kama vile mnavyoniona nilivyo." **40** [[Naye alipokuwa akisema hilo akawaonyesha mikono yake na miguu yake.]] **41** Lakini walipokuwa bado hawaamini[f] kwa ajili ya shangwe tupu na wakiwa wamestaajabu, akawaambia: "Je, mna chakula hapo?"[g] **42** Nao wakampa kipande cha samaki wa kuchomwa;[h] **43** naye akakichukua, akala[i] mbele ya macho yao.

44 Sasa akawaambia: "Haya ndiyo maneno yangu niliyowaambia nilipokuwa ningali

pamoja nanyi,[a] kwamba mambo yote yaliyoandikwa katika sheria ya Musa na katika Manabii[b] na Zaburi[c] juu yangu lazima yatimizwe." **45** Ndipo akafungua akili zao ili kuifahamu maana ya Maandiko,[d] **46** naye akawaambia: "Katika njia hii imeandikwa kwamba Kristo angeteseka na kufufuliwa kutoka kati ya wafu siku ya tatu,[e] **47** na kwa msingi wa jina lake toba kwa msamaha wa dhambi[f] ingehubiriwa katika mataifa yote[g]—kuanzia Yerusalemu,[h] **48** ninyi mnapaswa kuwa mashahidi[i] wa mambo haya. **49** Na, tazameni! ninatuma juu yenu kile ambacho kimeahidiwa na Baba yangu. Ingawa hivyo, ninyi kaeni katika jiji mpaka mvikwe nguvu kutoka juu."[a]

50 Lakini akawaongoza wende mpaka Bethania, naye akainua mikono yake na kuwabariki.[b] **51** Alipokuwa akiwabariki akatenganishwa nao, akaanza kuchukuliwa juu mbinguni.[c] **52** Nao wakamsujudia na kurudi Yerusalemu kwa shangwe kubwa.[d] **53** Nao sikuzote walikuwa katika hekalu wakimbariki Mungu.[e]

SURA 24
a Mt 16:21; Lu 9:22; Yoh 5:39
b Lu 24:27
c Zb 2:2; Zb 16:10; Zb 27:12; Zb 69:9; Zb 78:2; Zb 118:22; Zb 132:11
d Yoh 12:16
e Isa 53:5; Ho 6:2; Yon 1:17; Mk 9:31
f Mdo 5:31; Mdo 13:38
g Mwa 22:18; 1Ko 15:12; Ga 3:14; 1Ti 3:16
h Mdo 4:2; Mdo 5:28
i Yoh 15:27; Mdo 1:8

Safu ya 2
a Yoe 2:28; Yoh 14:16; Mdo 1:4; Mdo 2:4

b Kum 33:1; c Mdo 1:9; d Yoh 14:28; Yoh 16:22; Mdo 1:10; Mdo 1:12; e Mdo 2:46.

KULINGANA NA

YOHANA

1 Hapo mwanzo[a] Neno[b] alikuwako, na Neno alikuwa pamoja na Mungu,[c] na Neno alikuwa mungu.[d] **2** Hapo mwanzo[e] huyo alikuwa pamoja na Mungu.[f] **3** Vitu vyote vilikuja kuwako kupitia kwake,[g] na bila yeye hakuna hata kitu kimoja kilichokuja kuwako.

Kile ambacho kimekuja kuwako **4** kupitia kwake kilikuwa uzima,[h] na uzima ndio uliokuwa nuru[i] ya wanadamu. **5** Na nuru inang'aa katika giza,[j] lakini giza halijaizidi nguvu.

6 Kulitokea mtu aliyetumwa awe mwakilishi wa Mungu:[k] jina lake lilikuwa Yohana.[l] **7** Mtu huyo alikuja kwa ajili ya ushahidi, ili atoe ushahidi[m] juu ya nuru,[n] kusudi watu wa namna zote wapate kuamini kupitia kwake.[a] **8** Yeye hakuwa nuru hiyo,[b] bali alikusudiwa atoe ushahidi[c] juu ya nuru hiyo.

9 Nuru[d] ya kweli ambayo humpa nuru[e] mtu wa kila namna,[f] ilikuwa karibu kuja ulimwenguni. **10** Alikuwa ulimwenguni,[g] nao ulimwengu ulikuja kuwako kupitia kwake,[h] lakini ulimwengu haukumjua. **11** Alikuja nyumbani kwake mwenyewe, lakini watu wake mwenyewe hawakumkaribisha.[i] **12** Hata hivyo, wengi kadiri ileile waliompokea,[j] aliwapa mamlaka ya kuwa watoto

SURA 1
a Mt 8:22; Kol 1:15; Ufu 3:14
b Yoh 12:50; Ufu 19:13
c Mt 8:30; Yoh 17:5
d Isa 9:6; Yoh 1:18; Yoh 10:35; Flp 2:6
e Mwa 1:1; Mik 5:2
f Mwa 1:26; Mwa 3:22
g Yoh 1:10; 1Ko 8:6; Kol 1:16; Ebr 1:2
h Yoh 5:26; Mdo 3:15; 1Yo 1:2; 1Yo 5:11
i Yoh 8:12
j Yoh 3:19; Yoh 12:35
k Lu 3:2
l Mt 3:1; Lu 1:13
m Isa 40:3; Yoh 5:33
n Mt 3:11

Safu ya 2 a Mdo 19:4; b Yoh 1:20; Mdo 13:25; c Yoh 5:36; d Mt 4:16; Yoh 3:19; 1Yo 2:8; e Yoh 9:39; Yoh 12:46; f Mdo 13:47; g Yoh 1:14; h Yoh 1:3; i Lu 19:14; j Ro 9:27.

wa Mungu,[a] kwa sababu wali-
kuwa wakionyesha imani kati-
ka jina lake;[b] **13** nao walizali-
wa, si kutokana na damu au ku-
tokana na mapenzi ya mwili au
kutokana na mapenzi ya mwa-
nadamu, bali kutokana na Mu-
ngu.[c]

14 Kwa hiyo Neno akawa
mwili,[d] akakaa katikati yetu,
nasi tukautazama utukufu
wake, utukufu kama ule ulio wa
mwana mzaliwa-pekee[e] kutoka
kwa baba; naye alikuwa ame-
jaa fadhili nyingi zisizostahili-
wa na kweli.[f] **15** (Yohana ali-
toa ushahidi juu yake, ndiyo,
kwa kweli alipaaza sauti—huyu
ndiye aliyesema hilo—akise-
ma: "Yule anayekuja nyuma
yangu amekwenda mbele ya-
ngu, kwa sababu alikuwako
kabla yangu.")[g] **16** Kwa maa-
na sisi sote tulipokea kutokana
na wingi alio nao,[h] hata fadhi-
li zisizostahiliwa juu ya fadhi-
li zisizostahiliwa.[i] **17** Kwa sa-
babu Sheria ilitolewa kupitia
Musa,[j] fadhili zisizostahiliwa[k]
na kweli[l] zilikuja kupitia Yesu
Kristo. **18** Hakuna mwana-
damu ambaye amemwona Mu-
ngu wakati wowote;[m] mungu
mzaliwa-pekee[n] aliye kifuani[o]
pa Baba, ndiye ambaye amee-
leza juu yake.[p]

19 Basi huu ndio ushahidi
wa Yohana wakati Wayahu-
di walipowatuma makuhani na
Walawi kutoka Yerusalemu wa-
kamuulize: "Wewe ni nani?"[q]
20 Naye alikiri wala hakuka-
na, bali akakiri: "Mimi siye Kri-
sto."[r] **21** Nao wakamuuliza:
"Wewe ni nani, basi? Je, wewe
ndiye Eliya?"[s] Naye akasema:
"Mimi siye." "Je, wewe ndi-
ye Yule Nabii?"[t] Naye akajibu:
"Hapana!" **22** Kwa hiyo wa-
kamwambia: "Wewe ni nani? ili
tupate kuwajibu wale waliotu-
tuma. Unasema nini juu yako
mwenyewe?"[a] **23** Akasema:
"Mimi ni sauti ya mtu anayepa-
aza sauti nyikani, 'Nyoosheni
njia ya Yehova,' kama vile nabii
Isaya alivyosema."[b] **24** Sasa
wale waliotumwa walikuwa
wametoka kwa Mafarisayo.
25 Kwa hiyo walimuuliza na
kumwambia: "Kwa nini, basi,
unabatiza[c] ikiwa wewe mwe-
nyewe siye Kristo au Eliya au
Yule Nabii?" **26** Yohana aka-
wajibu, akisema: "Mimi ninaba-
tiza katika maji. Kuna mmo-
ja ambaye amesimama katika-
ti[d] yenu msiyemjua,[e] **27** yule
anayekuja nyuma yangu, lakini
ambaye kamba ya kiatu chake
sistahili kuifungua."[f] **28** Mam-
bo hayo yalitendeka Betha-
nia ng'ambo ya Yordani, amba-
ko Yohana alikuwa akibatizia.[g]

29 Siku iliyofuata alimwona
Yesu akimjia, naye akasema:
"Ona, Mwana-Kondoo[h] wa
Mungu ambaye huondolea
mbali dhambi[i] ya ulimwengu!
30 Huyu ndiye niliyesema juu
yake, Nyuma yangu anakuja
mwanamume ambaye yuko
mbele yangu, kwa sababu alikuwako kabla yangu.[k] **31** Hata
sikumjua, lakini nilikuja nikibatiza katika maji ili apate kufunuliwa kwa Israeli."[l] **32** Yohana pia alitoa ushahidi, akisema:
"Niliona roho ikishuka kama
njiwa kutoka mbinguni, nayo
ikakaa juu yake.[m] **33** Hata sikumjua, bali Yule aliyenituma[n]
nibatize katika maji aliniambia,

SURA 1

a Ro 8:16
2Ko 6:18
Efe 1:5
1Yo 3:1
b Ga 3:26
c Yoh 3:3
Yak 1:18
1Pe 1:23
1Yo 3:9
d Flp 2:7
1Ti 3:16
Ebr 2:14
1Yo 4:2
2Yo 7
e Yoh 3:16
1Yo 4:9
f Efe 4:21
g Lu 3:16
Yoh 8:58
Kol 1:17
h Kol 1:19
Kol 2:3
Kol 2:9
i Efe 1:6
j Kut 31:18
Kum 4:44
Yoh 7:19
k Ro 3:24
Ro 6:14
l Yoh 8:32
Yoh 14:6
Yoh 18:37
2Ko 1:20
m Kut 33:20
Yoh 6:46
1Yo 4:12
n Yoh 1:1
o Met 8:30
Yoh 13:23
p Mt 11:27
Lu 10:22
1Yo 3:2
q Lu 3:15
r Yoh 3:28
Mdo 13:25
s Mal 4:5
Mt 11:14
Mt 17:10
Mk 9:13
t Kum 18:15
Yoh 6:14
Yoh 7:40
Mdo 3:22

Safu ya 2

a Lu 3:16
b Isa 40:3
Mt 3:3
Lu 1:17
Lu 1:76
Lu 7:27
Yoh 3:28
c Mt 21:25
d Lu 17:21
e Isa 53:2
f Mt 3:11
Mdo 13:25
g Mt 3:6
h Kut 12:3
Isa 53:7
1Ko 5:7
1Pe 1:19
Ufu 5:6
i Isa 53:11
1Ko 15:3
Ebr 9:14
1Pe 2:24
1Yo 3:5
j Yoh 6:51
1Yo 2:2
1Yo 4:14
k Yoh 1:15
Yoh 8:58
Kol 1:17

l Isa 40:3; Mal 3:1; Lu 1:76; Mdo 19:4; m Mt 3:16; Mk 1:10; Lu 3:22; n Lu 3:2.

'Yeyote yule ambaye utaona
roho ikishuka na kukaa juu
yake, huyo ndiye ambaye hu-
batiza katika roho takatifu.'[a]
34 Nami nimeona, na nimetoa
ushahidi kwamba huyo ndiye
Mwana wa Mungu."[b]
35 Tena siku iliyofuata Yoha-
na alikuwa amesimama na wa-
wili kati ya wanafunzi wake,
36 na alipomtazama Yesu aki-
tembea akasema: "Ona, Mwana-
Kondoo[c] wa Mungu!" **37** Na
wanafunzi hao wawili waka-
msikia akisema, nao wakamfu-
ata Yesu. **38** Ndipo Yesu aka-
geuka na, alipowaona wakimfu-
ata, akawaambia: "Mnatafuta
nini?" Wakamwambia: "Rabi,
(ambalo linapotafsiriwa humaa-
nisha, Mwalimu,) unakaa wapi?"
39 Akawaambia: "Njooni, nanyi
mtaona."[d] Basi wakaenda waka-
ona ni wapi alikokuwa akikaa,
nao wakakaa pamoja naye siku
hiyo; ilikuwa karibu saa kumi.
40 Andrea[e] ndugu ya Simoni
Petro alikuwa mmoja kati ya
wale wawili waliosikia aliyoya-
sema Yohana nao wakamfuaa
Yesu. **41** Kwanza huyu ali-
mpata ndugu yake mwenye-
we, Simoni, na kumwambia:
"Tumempata Masihi"[f] (amba-
lo linapotafsiriwa humaanisha,
Kristo).[g] **42** Akampeleka kwa
Yesu. Yesu alipomtazama[h] aka-
sema: "Wewe ni Simoni[i] mwa-
na wa Yohana;[j] utaitwa Kefa"
(ambalo linatafsiriwa Petro).[k]
43 Siku iliyofuata alitama-
ni kuondoka kwenda Galilaya.
Kwa hiyo Yesu akamkuta Fili-
po[l] na kumwambia: "Uwe mfu-
asi wangu."[m] **44** Basi Filipo
alikuwa mtu wa Bethsaida,[n]
kutoka jiji la Andrea na Pe-
tro. **45** Filipo akamkuta Na-
thanaeli[a] na kumwambia: "Tu-
mempata yule ambaye Musa,
katika Sheria,[b] na Manabii,[c]
aliandika juu yake, Yesu,
mwana wa Yosefu,[d] kutoka Na-
zareti." **46** Lakini Nathanae-
eli akamwambia: "Je, kitu ch-
ochote kilicho chema kinawe-
za kutoka Nazareti?"[e] Filipo
akamwambia: "Njoo uone."
47 Yesu akamwona Nathanae-
eli akimjia na kusema juu yake:
"Ona, Mwisraeli kwa uhaki-
ka, ambaye hamna udanganyi-
fu ndani yake."[f] **48** Nathana-
eli akamwambia: "Umepataje
kunijua?" Yesu akajibu, aka-
mwambia: "Kabla ya Filipo ku-
kuita, ulipokuwa chini ya mti-
ni, nilikuona." **49** Nathanae-
eli akamjibu: "Rabi, wewe ndiye
Mwana wa Mungu,[g] wewe ndiye
Mfalme[h] wa Israeli." **50** Yesu
akajibu, akamwambia: "Je, una-
amini kwa sababu nilikuambia
nilikuona chini ya mtini? Utao-
na mambo makubwa zaidi kuli-
ko haya." **51** Akazidi kumwa-
mbia: "Kwa kweli kabisa ni-
nawaambia ninyi, Mtaona mbi-
ngu imefunguliwa na malaika[i]
za Mungu wakipanda na kushu-
ka mpaka kwa Mwana wa bina-
damu."[j]

2 Basi siku ya tatu kuliku-
wa na karamu ya ndoa katika
Kana[k] ya Galilaya, na mama[l]
ya Yesu alikuwa huko. **2** Yesu
na wanafunzi wake walialikwa
pia kwenye karamu hiyo ya
ndoa.
3 Divai ilipopungua mama[m]
ya Yesu akamwambia: "Hawa-
na divai." **4** Lakini Yesu aka-
mwambia: "Nina nini nawe,
mwanamke?[n] Saa yangu ha-
ijafika bado."[o] **5** Mama yake

SURA 1
a Mt 3:11
Mdo 1:5
Mdo 2:4
b Mt 3:17
Yoh 5:33
c Mdo 8:32
Ufu 5:12
d Mt 8:20
2Ko 8:9
e Mt 4:18
f Da 9:25
Yoh 11:27
g Yoh 4:25
h Yoh 2:25
i Mt 10:2
Mdo 15:14
j Mt 16:17
Yoh 21:15
k Mt 16:18
Mk 3:16
Lu 6:14
l Mt 10:3
m Mt 9:9
Ufu 14:4
n Mk 8:22
Yoh 12:21

Safu ya 2
a Mt 10:3
Lu 6:14
b Mwa 3:15
Mwa 22:18
Mwa 49:10
Kum 18:18
Yoh 5:46
c Isa 9:6
Yer 33:15
Eze 34:23
Mik 5:2
Zek 6:12
Mal 3:1
d Mt 1:16
Mt 13:55
Lu 2:4
e Yoh 7:41
f Yoh 2:25
g Lu 1:32
h Zek 9:9
Mt 27:11
Yoh 12:13
i Zb 104:4
Mt 4:11
Lu 22:43
j Mwa 28:12
Da 7:13

SURA 2
k Yoh 4:46
Yoh 21:2
l Lu 2:51
m Mdo 1:14
n Yoh 19:26
o Mt 26:2
Yoh 7:6
Yoh 12:23

akawaambia wale wenye kuhudumia: "Lolote atakalowaambia, fanyeni."[a] **6** Kama ilivyokuwa, kulikuwako mitungi sita ya maji ikiwa imekaa hapo kulingana na kanuni za utakaso[b] za Wayahudi, kila mmoja ukiwa unaweza kuchukua vipimo viwili au vitatu vya maji. **7** Yesu akawaambia: "Ijazeni maji mitungi ya maji." Nao wakaijaza pomoni. **8** Akawaambia: "Choteni kiasi fulani sasa na kumpelekea msimamizi wa karamu." Kwa hiyo wakayapeleka. **9** Basi, msimamizi wa karamu alipoyaonja maji yaliyokuwa yamegeuzwa kuwa divai,[c] lakini hakujua chanzo chake, ijapokuwa wale wenye kuhudumia waliokuwa wamechota hayo maji walijua, msimamizi wa karamu akamwita bwana-arusi **10** na kumwambia: "Wengine wote hutoa divai nzuri kwanza,[d] na ile hafifu wakati ambapo watu wameingiwa na kileo. Wewe umehifadhi divai nzuri mpaka sasa." **11** Yesu alifanya jambo hilo katika Kana ya Galilaya likiwa mwanzo wa ishara zake, naye akaufunua utukufu[e] wake; na wanafunzi wake wakamwamini.

12 Baada ya hayo, yeye na mama yake na ndugu zake[f] na wanafunzi wake wakashuka kwenda Kapernaumu,[g] lakini hawakukaa huko siku nyingi.

13 Basi pasaka[h] ya Wayahudi ilikuwa karibu, na Yesu akapanda kwenda Yerusalemu.[i] **14** Naye akakuta hekaluni wale waliokuwa wakiuza ng'ombe na kondoo na njiwa[j] na waliokuwa wakivunja pesa wakiwa wameketi. **15** Kwa hiyo, baada ya kufanya mjeledi wa kamba, akawafukuza hekaluni wale wote wenye kondoo na ng'ombe, akamwaga sarafu za waliokuwa wakibadili pesa na kupindua meza zao.[a] **16** Akawaambia wale waliokuwa wakiuza njiwa: "Ondoeni vitu hivi kutoka hapa! Acheni kuifanya nyumba[b] ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara!"[c] **17** Wanafunzi wake wakakumbuka kwamba imeandikwa: "Bidii kwa ajili ya nyumba yako itanila."[d]

18 Kwa hiyo, Wayahudi wakajibu, wakamwambia: "Una ishara[e] gani ya kutuonyesha, kwa kuwa unafanya mambo haya?" **19** Yesu akajibu, akawaambia: "Libomoeni hekalu[f] hili, na katika siku tatu nitalisimamisha." **20** Kwa hiyo Wayahudi wakasema: "Hekalu hili lilijengwa kwa miaka 46, nawe je, utalisimamisha katika siku tatu?" **21** Lakini alikuwa akiongea juu ya hekalu[g] la mwili wake. **22** Ingawa hivyo, wakati alipofufuliwa kutoka kwa wafu, wanafunzi wake wakakumbuka[h] kwamba alikuwa akisema hilo; nao wakaamini Andiko na maneno ambayo Yesu alisema.

23 Hata hivyo, wakati alipokuwa Yerusalemu kwenye pasaka, kwenye sherehe[i] yake, watu wengi wakawa na imani katika jina lake,[j] wakitazama ishara zake alizokuwa akifanya.[k] **24** Lakini Yesu mwenyewe hakuwa akiwatumaini[l] kwa sababu aliwajua wote **25** na kwa sababu hakuwa na uhitaji wa mtu yeyote kutoa ushahidi juu ya mwanadamu,

SURA 2

a Mwa 41:55
b Mk 7:3
Yoh 3:25
c Yoh 4:46
d Lu 5:39
e Isa 9:1
Yoh 1:14
f Mt 12:46
Mt 13:55
Mk 3:31
Lu 8:19
Mdo 1:14
1Ko 9:5
Ga 1:19
g Mt 4:13
h Kut 12:14
Hes 28:16
Kum 16:1
Yoh 11:55
Yoh 12:1
i Yoh 5:1
j Law 1:14

Safu ya 2

a Mt 21:12
Mk 11:15
Lu 19:45
b Zb 93:5
Lu 2:49
c Yer 7:11
Mt 21:13
Mk 11:17
Lu 19:46
d Zb 69:9
e Mt 12:38
Mt 16:1
Yoh 4:48
Yoh 6:30
f Mt 26:61
Mt 27:40
Mk 14:58
g Mt 12:6
Mt 16:21
Lu 24:7
1Ko 6:19
h Lu 24:8
Yoh 12:16
Yoh 14:26
Yoh 20:9
i Yoh 4:45
j Yoh 11:48
k Yoh 7:31
l Yoh 6:15

kwa maana yeye mwenyewe
alijua kile kilichokuwa ndani
ya mwanadamu.[a]

3 Basi kulikuwa na mtu
mmoja kati ya Mafarisa-
yo, aliyeitwa Nikodemo,[b] mta-
wala wa Wayahudi. **2** Huyo
alimjia wakati wa usiku[c] na ku-
mwambia: "Rabi,[d] tunajua kwa-
mba wewe ukiwa mwalimu[e]
umekuja kutoka kwa Mungu;[f]
kwa maana hakuna anayewe-
za kufanya ishara[g] hizi amba-
zo unafanya isipokuwa Mungu
awe pamoja naye."[h] **3** Yesu
akajibu akamwambia:[i] "Kwa
kweli kabisa ninakuambia, Mtu
asipozaliwa tena,[j] hawezi kuuo-
na ufalme wa Mungu."[k] **4** Ni-
kodemo akamwambia: "Mtu
anawezaje kuzaliwa akiwa
mzee? Je, anaweza kuingia ka-
tika tumbo la uzazi la mama
yake mara ya pili na kuzaliwa?"
5 Yesu akajibu: "Kwa kweli ka-
bisa ninakuambia, Mtu asipo-
zaliwa kwa maji[l] na roho,[m] ha-
wezi kuingia katika ufalme wa
Mungu. **6** Kile ambacho ki-
mezaliwa kwa mwili ni mwi-
li, na kile ambacho kimeza-
liwa kwa roho ni roho.[n] **7** Usi-
staajabu kwa sababu nimeku-
ambia, Ninyi lazima mzaliwe
tena.[o] **8** Upepo[p] huvuma ma-
hali ambapo unataka, nawe
unasikia mvumo wake, lakini
hujui mahali ambapo huo una-
toka wala mahali unapoenda.
Ndivyo alivyo kila mtu ambaye
amezaliwa kwa roho."[q]
9 Nikodemo akajibu, aka-
mwambia: "Mambo haya ya-
naweza kutukia jinsi gani?"
10 Yesu akajibu, akamwa-
mbia: "Je, wewe ni mwalimu
wa Israeli na bado hujui ma-
mbo haya?[a] **11** Kwa kweli ka-
bisa ninakuambia, Yale tuna-
yoyajua tunayasema na yale
ambayo tumeyaona tunatoa
ushahidi[b] juu yake, lakini ni-
nyi hampokei ushahidi ambao
tunatoa.[c] **12** Ikiwa nimewaam-
bia ninyi mambo ya duniani
na bado hamwamini, mtaami-
ni jinsi gani nikiwaambia ma-
mbo ya mbinguni?[d] **13** Zaidi
ya hayo, hakuna mtu amba-
ye amepanda kuingia mbingu-
ni[e] ila yule aliyeshuka kutoka
mbinguni,[f] Mwana wa binada-
mu.[g] **14** Na kama vile Musa
alivyoinua nyoka[h] nyikani, ndi-
vyo Mwana wa binadamu ata-
kavyoinuliwa,[i] **15** ili kila mtu
anayemwamini apate kuwa na
uzima wa milele.[j]
16 "Kwa maana Mungu ali-
upenda[k] ulimwengu sana hivi
kwamba akamtoa Mwana wake
mzaliwa-pekee,[l] ili kila mtu ana-
yemwamini[m] asiangamizwe[n]
bali awe na uzima wa milele.[o]
17 Kwa maana Mungu alimtu-
ma Mwana wake ulimwengu-
ni, si ili auhukumu[p] ulimwengu,
bali ili ulimwengu uokolewe[q]
kupitia kwake. **18** Yule ana-
yemwamini hatahukumiwa.[r]
Yule ambaye hamwamini ame-
hukumiwa tayari, kwa sababu
hana imani katika jina la Mwa-
na mzaliwa-pekee wa Mungu.[s]
19 Basi huu ndio msingi wa
hukumu, kwamba nuru[t] ime-
kuja ulimwenguni[u] lakini watu
wamelipenda giza kuliko nuru,[v]
kwa maana matendo yao ya-
likuwa maovu. **20** Kwa ma-
ana yule ambaye huzoea ku-

SURA 2
a Mt 9:4
Mk 2:8
Yoh 1:48
Yoh 6:64
Ufu 2:23

SURA 3
b Yoh 7:50
Yoh 19:39
c Yoh 12:42
d Yoh 1:38
e Mt 7:29
Yoh 7:46
f Yoh 7:16
Yoh 8:28
g Yoh 2:11
h Yoh 14:11
Mdo 2:22
Mdo 10:38
i Mdo 2:28
j Yoh 1:13
2Ko 5:17
Ga 6:15
1Pe 1:3
1Pe 1:23
1Yo 3:9
k 1Ko 15:50
l Mt 28:19
Mdo 8:36
Mdo 10:47
Mdo 19:5
m Mt 3:11
Yoh 1:33
Mdo 1:5
Mdo 10:45
Mdo 11:16
Mdo 19:6
1Ko 12:13
n 1Ko 15:44
o 1Pe 1:3
1Pe 1:23
p Mhu 11:5
q Yoh 14:17
Mdo 2:2
Ro 8:16
1Ko 2:11

Safu ya 2
a Yoh 9:30
b Yoh 8:26
c Yoh 3:32
1Ko 2:14
d Lu 22:67
e Mdo 2:34
Ebr 9:8
f Yoh 6:38
Yoh 8:23
Yoh 8:42
1Ko 15:47
Efe 4:9
g Yoh 1:51
h Hes 21:9
i Yoh 8:28
Ga 3:13
j Yoh 3:36
Yoh 20:31
k 1Yo 4:10
1Yo 4:19
l Mwa 22:2
Mwa 22:16
Ro 5:8
Ro 8:32
1Yo 4:9
m Yoh 1:12
Yoh 12:44
Efe 4:5
Flp 1:29
2Ti 3:15

n Mt 25:46; o Yoh 6:40; Yoh 20:31; Ro 6:23; 1Yo 5:13; p Yoh 12:47; 2Ko 5:19; q Lu 19:10; 1Ko 15:22; 1Ti 1:15; 1Yo 2:2; 1Yo 4:14; r Yoh 5:24; Ro 8:1; s Mt 10:33; Ebr 10:29; t Yoh 1:9; Yoh 8:12; Yoh 9:5; Yoh 12:46; u Yoh 1:5; v Ayu 24:13; Isa 5:20; Yoh 12:48.

fanya mambo maovu[a] huchukia
nuru na haji kwenye nuru, ili
matendo yake yasipate kukari-
piwa.[b] **21** Lakini yule amba-
ye hufanya yaliyo ya kweli huja
kwenye nuru,[c] ili matendo yake
yapate kufunuliwa kuwa ta-
yari yamefanywa kupatana na
Mungu."

22 Baada ya mambo haya
Yesu na wanafunzi wake waka-
enda katika nchi ya Yudea, na
huko akatumia wakati fulani
pamoja nao naye alikuwa aki-
batiza.[d] **23** Lakini Yohana[e]
pia alikuwa akibatiza katika
Ainoni karibu na Salimu, kwa
sababu kulikuwa na kiasi kiku-
bwa cha maji[f] huko, na watu
wakawa wakija na kubatizwa;[g]
24 kwa maana Yohana alikuwa
hajatupwa gerezani bado.[h]

25 Kwa hiyo bishano likato-
kea kati ya wanafunzi wa Yo-
hana na Myahudi mmoja ku-
husu utakaso.[i] **26** Kwa hiyo
wakaja kwa Yohana na kumwa-
mbia: "Rabi, mtu aliyekuwa pa-
moja nawe ng'ambo ya Yorda-
ni, ambaye umetoa ushahidi[j]
juu yake, ona, huyu anabati-
za na wote wanamwendea."[k]
27 Yohana akajibu, akasema:
"Mtu hawezi kupokea hata kitu
kimoja isipokuwa awe amepe-
wa kutoka mbinguni.[l] **28** Ni-
nyi wenyewe mnanitolea usha-
hidi kwamba nilisema, Mimi
siye Kristo,[m] bali, nimetumwa
kumtangulia huyo.[n] **29** Yeye
aliye na bibi-arusi ndiye bwa-
na-arusi.[o] Hata hivyo, rafiki ya
bwana-arusi, anaposimama na
kumsikia, ana shangwe nyi-
ngi sana kwa sababu ya sau-
ti ya bwana-arusi. Kwa hiyo
shangwe yangu hii imejazwa.[p]
30 Lazima huyo aendelee kuo-
ngezeka, lakini mimi lazima ni-
endelee kupungua."

31 Yule anayekuja kutoka
juu yuko juu ya wengine wote.[a]
Yule anayetoka duniani ni wa
kutoka duniani na husema ku-
husu mambo ya duniani.[b] Yule
anayekuja kutoka mbinguni
yuko juu ya wengine wote.[c]
32 Kile ambacho ameona na
kusikia, yeye hutoa ushahidi
juu yake,[d] lakini hakuna mtu
anayekubali ushahidi wake.[e]
33 Yule ambaye ameukubali
ushahidi wake ametia muhuri
wake juu ya huo kwamba Mu-
ngu ni wa kweli.[f] **34** Kwa ma-
ana yule ambaye Mungu ame-
mtuma husema maneno ya Mu-
ngu,[g] kwa maana hatoi roho
kwa kipimio.[h] **35** Baba hu-
mpenda Mwana[i] naye ametia
vitu vyote mkononi mwake.[j]
36 Yule anayemwamini[k] Mwa-
na ana uzima wa milele;[l] yule
asiyemtii Mwana hataona uzi-
ma,[m] bali ghadhabu ya Mungu
hukaa juu yake.[n]

4 Basi, Bwana alipojua kwa-
mba Mafarisayo walikuwa
wamesikia kwamba Yesu aliku-
wa akifanya na kubatiza[o] wa-
nafunzi wengi kuliko Yohana—
2 ijapokuwa, kwa kweli, Yesu
mwenyewe hakuwa akibatiza
ila wanafunzi wake ndio wa-
liokuwa wakibatiza— **3** alio-
ndoka Yudea na kuelekea tena
Galilaya. **4** Lakini ilikuwa la-
zima apitie Samaria.[p] **5** Basi
akaja mpaka jiji moja la Sa-
maria linaloitwa Sikari kari-
bu na shamba ambalo Yakobo
alimpa Yosefu mwana wake.[q]
6 Kwa kweli, chemchemi[r] ya
Yakobo ilikuwa hapo. Basi

SURA 3
a 1Ko 6:9
Ga 5:19
1Pe 4:3
b Efe 5:13
c Yoh 12:36
Yoh 12:46
1Yo 1:7
d Yoh 3:26
Yoh 4:2
e Mt 3:1
f Mk 1:10
Mdo 8:36
g Mt 3:6
h Mt 14:3
Lu 3:20
i Mk 7:3
j Yoh 1:7
Yoh 1:34
k Yoh 6:65
l Yoh 19:11
Ebr 5:4
Yak 1:17
m Yoh 1:20
Mdo 13:25
n Isa 40:3
Mal 3:1
Mt 11:10
Lu 1:17
o Mt 22:2
2Ko 11:2
Efe 5:25
Ufu 21:9
p Lu 1:44

Safu ya 2
a Yoh 8:23
b 1Yo 4:5
c Mt 3:11
d Yoh 8:26
Yoh 15:15
e Isa 53:2
Yoh 1:11
Yoh 3:11
f Ro 3:4
1Yo 5:10
g Yoh 7:16
h Yoh 1:16
i Yoh 5:20
Yoh 15:9
j Mt 11:27
Mt 28:18
Lu 10:22
Yoh 17:2
k Hab 2:4
Ro 1:17
l Yoh 3:16
Yoh 6:47
Ebr 5:9
m 2Th 1:8
1Yo 5:12
n Ro 2:8
Efe 5:6
Ebr 10:27

SURA 4
o Yoh 3:22
p Lu 9:52
q Mwa 33:19
Mwa 48:22
Yos 24:32
r Yoh 4:12

Yesu, kwa kuwa alikuwa amechoka kwa sababu ya safari
hiyo, alikuwa ameketi kando ya
chemchemi kama vile alivyo-
kuwa. Ilikuwa karibu saa sita.
7 Mwanamke mmoja wa Sa-
maria akaja kuteka maji. Yesu
akamwambia: "Nipe maji ni-
nywe." **8** (Kwa maana wana-
funzi wake walikuwa wamee-
nda katika jiji kununua chaku-
la.) **9** Kwa hiyo mwanamke
huyo Msamaria akamwambia:
"Wewe, ujapokuwa Myahudi,
unawezaje kuniomba maji ya
kunywa, na mimi ni mwana-
mke Msamaria?" (Kwa maa-
na Wayahudi hawana shughu-
li na Wasamaria.)[a] **10** Yesu
akajibu, akamwambia: "Kama
ungalijua zawadi[b] ya bure ina-
yotoka kwa Mungu, na ni nani[c]
ambaye anakuambia, 'Nipe
maji ninywe,' ungalimwo-
mba, naye angalikupa maji ya-
liyo hai."[d] **11** Akamwambia:
"Bwana, huna hata ndoo ya ku-
tekea maji, na kisima ni kirefu.
Kwa hiyo, umeyatoa wapi maji
hayo yaliyo hai? **12** Je, wewe
ni mkuu[e] kuliko babu yetu Ya-
kobo, ambaye alitupa kisima
hiki na ambaye yeye mwenye-
we pamoja na wanawe na mi-
fugo yake walikunywa maji
yake?" **13** Yesu akajibu, aka-
mwambia: "Kila mtu anayeku-
nywa maji haya atapatwa na
kiu tena. **14** Yule atakayeku-
nywa maji ambayo nitampa ha-
tapatwa na kiu hata kidogo,[f] la-
kini maji ambayo nitampa ya-
takuwa chemchemi ya maji[g]
ndani yake, inayobubujika ili
kutokeza uzima wa milele."[h]
15 Huyo mwanamke akamwa-
mbia: "Bwana, nipe maji hayo,

SURA 4
a 2Fa 17:24
Ezr 4:3
Lu 9:52
Mdo 10:28
b Efe 2:8
c Isa 9:6
Yoh 4:26
d Isa 12:3
Yer 2:13
Zek 13:1
Zek 14:8
Yoh 7:37
e Mt 12:41
Lu 11:31
Yoh 8:53
f Yoh 6:35
Yoh 7:38
g Isa 58:11
h Ro 6:23
1Yo 5:20

Safu ya 2
a Lu 7:16
Lu 7:39
Yoh 9:17
b Kum 11:29
c Kum 12:5
1Fa 9:3
2Nya 7:12
Zb
122:Uta-9
d Mal 1:11
e Mk 14:58
Ebr 9:11
f 2Fa 17:29
2Fa 17:33
g Isa 2:3
Ro 9:4
h Yoh 14:17
Ro 8:4
2Ko 4:18
2Ko 5:7
Flp 3:3
i Yos 24:14
1Sa 12:24
Zb 25:5
Zb 86:11
Mk 7:7
j 2Nya 16:9
k 2Ko 3:17
1Ti 1:17
Ebr 11:27
l Ro 12:1
m Kum 18:18
Da 9:25
Yoh 1:41
n Yoh 11:27
o Yoh 9:37

ili nisiwe na kiu wala nisiende-
lee kuja hapa kuteka maji."
16 Akamwambia: "Nenda,
ukamwite mume wako mje
hapa." **17** Mwanamke huyo
akajibu akasema: "Sina mume."
Yesu akamwambia: "Umesema
vema, 'Sina mume.' **18** Kwa
maana umekuwa na waume wa-
tano, na mwanamume uliye naye
sasa si mume wako. Hapo ume-
sema kweli." **19** Huyo mwana-
mke akamwambia: "Bwana, ni-
naona kwamba wewe ni na-
bii.[a] **20** Mababu zetu waliabu-
du katika mlima huu;[b] lakini
ninyi husema kwamba Yeru-
salemu ndipo mahali ambapo
watu wanapaswa kuabudia."[c]
21 Yesu akamwambia: "Niami-
ni mimi, mwanamke, Saa ina-
kuja wakati ambapo mtamwa-
budu[d] Baba si katika mlima
huu wala kule Yerusalemu.[e]
22 Ninyi mnaabudu msichoki-
jua; sisi tunaabudu tunachoki-
jua,[f] kwa sababu wokovu huto-
kana na Wayahudi.[g] **23** Hata
hivyo, saa inakuja, nayo ipo
sasa, wakati ambapo waabudu
wa kweli watamwabudu Baba
kwa roho[h] na kweli,[i] kwa maa-
na, kwa kweli, Baba anawatafu-
ta watu wa namna hiyo wamwa-
budu.[j] **24** Mungu ni Roho,[k] na
wale wanaomwabudu lazima
wamwabudu kwa roho na kwe-
li."[l] **25** Huyo mwanamke aka-
mwambia: "Ninajua kwamba
Masihi[m] anakuja, anayeitwa
Kristo.[n] Atakapofika, atatu-
julisha mambo yote waziwazi."
26 Yesu akamwambia: "Mimi
ninayesema nawe ndiye."[o]
27 Ndipo wanafunzi wake
wakafika, nao wakaanza ku-
staajabu kwa sababu aliku-

wa akisema na mwanamke.
Bila shaka, hakuna yeyote aliyesema: "Unatafuta nini?" au,
"Kwa nini unaongea naye?"
28 Kwa hiyo, mwanamke huyo
akauacha mtungi wake wa maji
akaenda zake jijini na kuwaa-
mbia watu: **29** "Njooni hapa,
mwone mtu aliyeniambia ma-
mbo yote niliyofanya. Je, huyu
labda ndiye Kristo?"[a] **30** Wa-
katoka jijini na kumwendea.

31 Wakati huohuo wana-
funzi walikuwa wakimhimiz-
a, wakisema: "Rabi,[b] kula."
32 Lakini akawaambia: "Mimi
nina chakula ambacho hamki-
jui." **33** Kwa hiyo wanafunzi
wakaanza kusemezana: "Je,
kuna mtu ambaye amemletea
chakula chochote?" **34** Yesu
akawaambia: "Chakula[c] cha-
ngu ni mimi kufanya mapenzi[d]
yake aliyenituma na kuimali-
za kazi yake.[e] **35** Je, ninyi ha-
msemi kwamba bado kuna mi-
ezi minne kabla ya mavuno
kuja? Tazama! Ninawaambia
ninyi: Inueni macho yenu mya-
tazame mashamba, kwamba ni
meupe kwa ajili ya kuvunwa.[f]
Tayari **36** mvunaji anapokea
mshahara na kukusanya ma-
tunda kwa ajili ya uzima wa
milele,[g] ili mpandaji[h] na mvu-
naji wapate kushangilia pamo-
ja.[i] **37** Katika habari hii, kwa
kweli, maneno haya ni kweli,
Mpandaji ni mmoja na mvunaji
ni mwingine. **38** Niliwatuma
ninyi mkavune kile ambacho
hamkufanyia kazi. Wengine
wamefanya kazi,[j] nanyi mmei-
ngia katika faida ya kazi yao."

39 Sasa wengi wa Wasama-
ria kutoka jiji hilo walimwami-
ni[k] kwa sababu ya neno la yule
mwanamke aliyesema hivi kwa
ushahidi: "Aliniambia mambo
yote niliyofanya."[a] **40** Kwa
hiyo Wasamaria walipomjia,
wakaanza kumwomba akae pa-
moja nao; naye akakaa huko
siku mbili.[b] **41** Kwa hiyo
wengi zaidi wakaamini kwa
ajili ya aliyoyasema,[c] **42** nao
wakaanza kumwambia yule
mwanamke: "Hatuamini tena
kwa sababu ya maneno yako;
kwa maana sisi wenyewe[d] tu-
mesikia nasi tunajua kwamba
mtu huyu kwa hakika ndiye
mwokozi[e] wa ulimwengu."

43 Baada ya hizo siku mbili
akaondoka huko kwenda Gali-
laya.[f] **44** Hata hivyo, Yesu ali-
toa ushahidi kwamba nabii ha-
pati heshima katika nchi yake
mwenyewe.[g] **45** Kwa hiyo,
alipofika Galilaya, Wagalilaya
wakampokea, kwa sababu wa-
likuwa wameona mambo yote
aliyofanya Yerusalemu kwenye
sherehe,[h] kwa maana wao pia
walikuwa wameenda kwenye
sherehe.[i]

46 Basi akaja tena mpa-
ka Kana[j] ya Galilaya, amba-
ko alikuwa amegeuza maji
yakawa divai.[k] Basi kuliku-
wako mtumishi fulani wa mfa-
lme ambaye mwana wake ali-
kuwa mgonjwa katika Kaper-
naumu.[l] **47** Mtu huyu alipo-
sikia kwamba Yesu alikuwa
amekuja kutoka Yudea kuin-
gia Galilaya, akamwendea
na kuanza kumwomba ashu-
ke ili amponye mwana wake,
kwa maana alikuwa karibu
kufa. **48** Hata hivyo, Yesu
akamwambia: "Msipoona isha-
ra[m] na maajabu,[n] hamtaami-
ni kamwe." **49** Mtumishi wa
mfalme akamwambia: "Bwana,
shuka uje kabla mtoto wangu

SURA 4

a Kum 18:15
Yoh 7:26
b Yoh 1:38
c Mt 4:4
d Yoh 5:30
Yoh 6:38
e Yoh 5:36
Yoh 17:4
Yoh 19:30
f Mt 9:37
g Ro 6:22
h Met 11:18
i Da 12:3
1Ko 3:8
2Yo 8
j Mdo 10:43
1Pe 1:12
k Eze 16:53
Ro 10:17

Safu ya 2

a Yoh 4:29
b Mt 10:11
Mdo 10:48
c Yoh 10:27
d Yoh 17:8
e Isa 49:6
Mt 1:21
Yoh 1:29
Mdo 13:23
1Ti 1:15
1Yo 4:14
f Yoh 4:40
g Mt 13:57
Mk 6:4
Lu 4:24
h Yoh 2:23
i Kum 16:16
j Yoh 21:2
k Yoh 2:1
Yoh 2:11
l Mt 8:5
m Mt 16:1
Yoh 2:18
1Ko 1:22
n Mdo 4:30

mchanga hajafa.” **50** Yesu
akamwambia: “Shika njia uende zako;[a] mwana wako yuko
hai.”[b] Yule mtu akaliamini neno
ambalo Yesu alikuwa amemwambia, akashika njia na kwenda zake. **51** Lakini tayari
alipokuwa akishuka kwenda
zake watumwa wake wakakutana naye ili kusema kwamba
mvulana wake alikuwa hai.[c]
52 Kwa hiyo akaanza kuwauliza saa ambayo alipata nafuu. Basi wakamwambia: “Jana
saa saba homa[d] ilimwacha.”
53 Kwa hiyo yule baba akajua ilikuwa saa[e] ileile ambayo Yesu alimwambia: “Mwana wako yuko hai.” Kisha yeye
na watu wote wa nyumbani
mwake wakaamini.[f] **54** Tena
hiyo ilikuwa ndiyo ishara[g] ya
pili aliyoifanya Yesu alipokuja
kutoka Yudea na kuingia Galilaya.

5 Baada ya mambo hayo kulikuwa na sherehe[h] ya Wa-
yahudi, na Yesu akapanda kwenda Yerusalemu. **2** Sasa katika Yerusalemu kwenye lango la
kondoo[i] kuna dimbwi linaloitwa
katika Kiebrania Bethzatha, lenye mistari mitano ya nguzo.
3 Hapo umati wa wagonjwa, vipofu, vilema na wale wenye viungo vilivyopooza, walikuwa wa-
melala chini. **4** —— **5** La-
kini kulikuwa na mtu fulani
hapo ambaye alikuwa mgonjwa
kwa miaka 38. **6** Alipomwona
mtu huyu amelala chini, na akiwa anajua kwamba tayari amekuwa mgonjwa muda mrefu,[j]
Yesu akamwambia: “Je, unataka
kuwa na afya nzuri?”[k] **7** Mgonjwa huyo akamjibu: “Bwana,
sina mtu wa kuniweka ndani ya

SURA 4
a Mt 8:13
Mk 7:29
b 1Fa 17:23
c Mk 7:30
d Mt 8:15
Mdo 28:8
e Mt 8:13
f Mdo 11:14
Mdo 18:8
g Yoh 2:11

SURA 5
h Kut 12:14
Kum 16:1
Kum 16:16
Yoh 2:13
Yoh 6:4
i Ne 3:1
Ne 12:39
j Lu 13:11
k Zb 72:13
Isa 53:3

Safu ya 2
a Mt 9:6
Mk 2:11
Lu 5:24
Mdo 3:7
b Yoh 9:14
c Kut 20:10
Ne 13:19
Yer 17:21
Mt 12:2
Lu 6:2
d Mt 12:14
Yoh 15:20
e Mwa 2:3
Yoh 9:4
Yoh 14:10
f Yoh 7:1
Yoh 7:19

dimbwi wakati maji yanapotibuliwa; lakini wakati ninapokuwa
nikija mwingine hushuka mbele
yangu.” **8** Yesu akamwambia:
“Simama, chukua kitanda cha-
ko, utembee.”[a] **9** Ndipo mtu
huyo akawa na afya nzuri mara
moja, naye akachukua kitanda
chake, akaanza kutembea.

Basi siku hiyo ilikuwa siku
ya sabato.[b] **10** Kwa hiyo Wa-
yahudi wakaanza kumwambia mtu huyo aliyeponywa:
“Ni Sabato, na si halali[c] uki-
chukue kitanda.” **11** Laki-
ni akawajibu: “Yule aliyenifanya niwe na afya nzuri aliniambia, ‘Chukua kitanda chako
utembee.’” **12** Wakamuuliza: “Ni nani huyo aliyekuambia, ‘Kichukue utembee’?”
13 Lakini mwanamume huyo
aliyeponywa hakujua alikuwa
nani, kwa maana Yesu alikuwa
amegeukia kando, mahali hapo
pakiwa pana umati.

14 Baada ya mambo haya
Yesu alimkuta hekaluni aka-
mwambia: “Ona, una afya nzuri. Usifanye dhambi tena ka-
mwe, ili usipatwe na jambo fu-
lani baya zaidi.” **15** Mtu yule
akaenda zake akawaambia Wayahudi kwamba Yesu ndiye aliyemfanya awe na afya nzuri.
16 Kwa hiyo Wayahudi waka-
mtesa[d] Yesu, kwa sababu ali-
kuwa akifanya mambo hayo
wakati wa siku ya Sabato.
17 Lakini akawajibu: “Baba ya-
ngu anaendelea kufanya kazi
mpaka sasa, na mimi ninaende-
lea kufanya kazi.”[e] **18** Kwa
kweli, kwa sababu hiyo Wayahudi wakaanza kutafuta hata
zaidi kumuua,[f] kwa sababu si
kwamba tu alikuwa akiivunja Sabato bali pia alikuwa

akimwita Mungu Baba[a] yake
mwenyewe, akijifanya mwe-
nyewe kuwa sawa[b] na Mungu.
19 Kwa hiyo, Yesu akajibu,
akawaambia: "Kwa kweli ka-
bisa ninawaambia ninyi, Mwa-
na hawezi kufanya hata jambo
moja kwa uamuzi wake mwe-
nyewe, ila tu lile analomwo-
na Baba akifanya.[c] Kwa maa-
na mambo yoyote yale amba-
yo Yule hufanya, mambo hayo
Mwana pia hufanya vivyo hi-
vyo. **20** Kwa maana Baba
anampenda Mwana[d] na hu-
mwonyesha mambo yote ana-
yofanya yeye mwenyewe, naye
atamwonyesha kazi zilizo ku-
bwa zaidi kuliko hizi, ili ninyi
mpate kustaajabu.[e] **21** Kwa
maana kama vile Baba anavyo-
wafufua wafu na kuwafanya
hai,[f] ndivyo Mwana pia anavyo-
wafanya hai wale anaotaka ku-
wafanya hai.[g] **22** Kwa maana
Baba hamhukumu mtu yeyote
hata kidogo, bali amemkabidhi
Mwana kazi yote ya kuhuku-
mu,[h] **23** ili wote wapate ku-
mheshimu Mwana[i] kama vile
wanavyomheshimu Baba. Yule
ambaye hamheshimu Mwana
hamheshimu Baba aliyemtu-
ma.[j] **24** Kwa kweli kabisa ni-
nawaambia ninyi, Yule ambaye
husikia neno langu na kumwa-
mini yule aliyenituma ana uzi-
ma wa milele,[k] naye haingii hu-
kumuni bali amevuka kutoka
katika kifo na kuingia katika
uzima.[l]
25 "Kwa kweli kabisa nina-
waambia ninyi, Saa inakuja,
nayo ipo sasa, wakati amba-
po wafu[m] wataisikia sauti[n]
ya Mwana wa Mungu na wale
ambao wamesikiliza wataishi.[o]

SURA 5
a Yoh 10:38
Yoh 14:28
b Flp 2:6
c Yoh 5:30
Yoh 8:28
Yoh 12:49
d Mt 3:17
Yoh 3:35
Yoh 10:17
2Pe 1:17
e Lu 8:25
Yoh 6:11
Yoh 6:19
f 2Fa 4:34
Ebr 11:35
g Lu 7:14
Lu 8:54
Yoh 11:25
Ufu 1:18
h Kut 18:13
Mt 11:27
Mdo 10:42
Mdo 17:31
2Ko 5:10
2Ti 4:1
i Yoh 3:35
Flp 2:10
j Lu 10:16
k Yoh 3:16
Yoh 6:40
Yoh 8:51
l 1Yo 3:14
m Mt 8:22
n Yoh 10:27
o Ro 6:13
Efe 2:5

Safu ya 2
a Zb 36:9
Mdo 17:28
b Yoh 11:25
Ufu 1:18
c Yoh 5:22
2Ti 4:1
d Da 7:13
e Ayu 14:13
Isa 25:8
Isa 26:19
Ufu 20:12
f Da 12:2
Ufu 20:12
g 2Pe 2:9
Ufu 20:15
h Isa 11:4
i Mt 26:39
Yoh 4:34
Yoh 6:38
j Kum 19:15
k Yoh 8:14
l Mt 3:17
Mk 9:7
Yoh 12:30
1Yo 5:9
m Yoh 1:15
Yoh 1:32
n Yoh 11:42
o Mt 3:5
Mt 13:20
Mk 6:20
2Pe 1:19

26 Kwa maana kama vile Baba
alivyo na uzima ndani yake
mwenyewe,[a] ndivyo pia ame-
mruhusu Mwana awe na uzi-
ma ndani yake mwenyewe.[b]
27 Naye amempa mamlaka ya
kuhukumu,[c] kwa sababu yeye
ndiye Mwana wa binadamu.[d]
28 Msistaajabie jambo hili,
kwa sababu saa inakuja amba-
yo wale wote waliomo ndani ya
makaburi ya ukumbusho[e] wa-
taisikia sauti yake **29** na ku-
toka, wale waliotenda mambo
mema kwenye ufufuo wa uzi-
ma,[f] wale waliokuwa na zoea
la kutenda mambo maovu kwe-
nye ufufuo wa hukumu.[g]
30 Mimi siwezi kufanya lolote
kwa uamuzi wangu mwenyewe;
kama vile ninavyosikia, ndivyo
ninavyohukumu; na hukumu
ninayotoa ni ya uadilifu,[h] kwa
sababu ninatafuta, si mapenzi
yangu mwenyewe, bali mape-
nzi[i] yake aliyenituma.
31 "Ikiwa mimi peke yangu
ninatoa ushahidi[j] juu yangu
mwenyewe, ushahidi wangu si
wa kweli.[k] **32** Kuna mwingi-
ne ambaye hutoa ushahidi juu
yangu, nami ninajua kwamba
ushahidi ambao yeye hutoa[l] juu
yangu ni wa kweli. **33** Ninyi
mmetuma watu kwa Yohana,
naye ametoa ushahidi kwa ile
kweli.[m] **34** Hata hivyo, mimi
siukubali ushahidi kutoka kwa
mwanadamu, bali ninasema
mambo hayo ili mpate kuoko-
lewa.[n] **35** Mtu huyo alikuwa
taa yenye kuwaka na yenye ku-
ng'aa, nanyi kwa wakati mfu-
pi mlikuwa na nia ya kusha-
ngilia sana katika nuru yake.[o]
36 Lakini mimi nina ushahidi
ulio mkubwa zaidi kuliko ule
wa Yohana, kwa maana kazi

zilezile ambazo Baba yangu alinigawia kutimiza, kazi hizo zenyewe ambazo ninafanya,[a] hutoa ushahidi juu yangu kwamba Baba alinituma. **37** Pia, Baba aliyenituma yeye mwenyewe ametoa ushahidi juu yangu.[b] Ninyi hamjasikia sauti yake wakati wowote wala kuona umbo lake;[c] **38** nanyi hamna neno lake likikaa ndani yenu, kwa sababu yuleyule ambaye yeye alimtuma ninyi hammwamini.

39 "Ninyi mnayachunguza Maandiko,[d] kwa sababu mnafikiri kwamba kwa njia yake mtakuwa na uzima wa milele; na hayo yenyewe ndiyo yanayotoa ushahidi juu yangu.[e] **40** Na bado hamtaki kuja kwangu ili mpate kuwa na uzima.[f] **41** Mimi siukubali utukufu kutoka kwa wanadamu,[g] **42** lakini ninajua vizuri kwamba ninyi hammpendi Mungu ndani yenu.[h] **43** Mimi nimekuja katika jina la Baba yangu,[i] lakini ninyi hamnipokei; ikiwa mtu mwingine angefika katika jina lake mwenyewe, mngempokea huyo. **44** Mtawezaje kuamini, wakati ninyi mnakubali utukufu[j] kutoka kwa mtu na mwenzake na hamtafuti utukufu unaotoka kwa Mungu wa pekee?[k] **45** Msifikiri kwamba nitawashtaki kwa Baba; kuna mmoja ambaye huwashtaki ninyi, Musa,[l] ambaye mmemtumaini. **46** Kwa kweli, ikiwa mngalimwamini Musa mngaliniamini mimi, kwa maana huyo aliandika juu yangu.[m] **47** Lakini ikiwa hamyaamini maandishi yake huyo,[n] mtawezaje kuyaamini maneno yangu?"

SURA 5
a Mt 11:5
Yoh 3:2
Yoh 7:31
Yoh 10:25
b Mt 17:5
Mk 1:11
Yoh 8:18
Yoh 12:30
1Yo 5:9
c Kum 4:12
Yoh 1:18
Yoh 6:46
1Ti 1:17
1Yo 4:12
d Isa 8:20
Lu 11:52
Mdo 17:11
2Ti 3:15
1Pe 1:10
e Kum 18:15
f Isa 53:3
Yoh 1:11
g 1Th 2:6
h 1Yo 4:20
i Kut 3:15
j Yoh 12:43
k 1Ko 4:5
l Kum 31:26
Yoh 7:19
Ro 2:12
m Mwa 3:15
Mwa 49:10
Kum 18:15
Lu 24:44
Yoh 1:45
Mdo 26:22
n Lu 16:31

Safu ya 2

SURA 6
a Mt 14:13
Lu 9:10
b Mk 6:33
Lu 9:11
Yoh 2:23
c Mt 15:29
d Yoh 2:13
Yoh 5:1
e Mt 14:14
Mk 6:35
Lu 9:12
f Mk 6:37
g 2Fa 4:42
h Mt 14:17
Mk 6:38
Lu 9:13
i Mwa 18:4
j 2Fa 4:43
Mt 14:19
Mt 14:21
Mk 6:39
Mk 6:44
Lu 9:14
k 2Fa 4:44
Mk 6:41
Lu 9:16
l Mk 6:42

6 Baada ya mambo haya Yesu akaondoka kwenda ng'ambo ya bahari ya Galilaya, au Tiberia.[a] **2** Lakini umati mkubwa wakamfuata, kwa sababu walikuwa wakiona ishara alizokuwa akifanya juu ya wale waliokuwa wakiugua.[b] **3** Kwa hiyo Yesu akapanda mlimani,[c] na hapo alikuwa ameketi pamoja na wanafunzi wake. **4** Sasa pasaka,[d] ile sherehe ya Wayahudi, ilikuwa karibu. **5** Kwa hiyo, Yesu alipoinua macho yake na kuona kwamba umati mkubwa walikuwa wakimjia, akamwambia Filipo: "Tutanunua wapi mikate ili hawa wale?"[e] **6** Hata hivyo, alikuwa akisema hilo ili amjaribu, kwa maana yeye mwenyewe alijua alilokuwa karibu kufanya. **7** Filipo akamjibu: "Mikate yenye thamani ya dinari mia mbili haiwatoshi, hata kwamba kila mmoja aweze kupata kidogo."[f] **8** Mmoja wa wanafunzi wake, Andrea ndugu ya Simoni Petro, akamwambia: **9** "Hapa yupo mvulana mdogo ambaye ana mikate mitano ya shayiri[g] na samaki wadogo wawili. Lakini vitu hivi ni nini kwa watu wengi sana hivi?"[h]

10 Yesu akasema: "Waketisheni watu kama kwenye mlo."[i] Basi kulikuwa na majani mengi hapo. Kwa hiyo wanaume wakaketi, hesabu yao karibu elfu tano.[j] **11** Basi Yesu akachukua ile mikate na, baada ya kushukuru, akaigawanya kwa wale waliokuwa wameketi, vivyo hivyo pia wale samaki wadogo kadiri walivyotaka.[k] **12** Lakini walipokuwa wameshiba[l] akawaambia wa-

nafunzi wake: "Kusanyeni pamoja vipande ambavyo vimebaki, ili chochote kisipotee bure."
13 Kwa hiyo wakavikusanya pamoja, nao wakajaza vikapu kumi na viwili kwa vipande vya mikate mitano ya shayiri, ambavyo vilibakizwa na wale waliokuwa wamekula.[a]

14 Kwa hiyo watu hao walipoona ishara alizofanya, wakaanza kusema: "Kwa hakika huyu ndiye nabii[b] aliyepaswa kuja ulimwenguni."
15 Kwa hiyo Yesu, akijua walikuwa karibu kuja kumkamata wamfanye kuwa mfalme, akaondoka[c] tena kwenda mlimani akiwa peke yake.

16 Kulipokuwa jioni, wanafunzi wake wakashuka kwenda baharini,[d] **17** na, baada ya kupanda mashua, wakaondoka kwenda ng'ambo ya bahari ili waende Kapernaumu. Basi, kufikia sasa, giza lilikuwa limeingia na Yesu alikuwa bado hajaja mahali walipokuwa. **18** Pia, bahari ikaanza kuchafuka kwa sababu upepo wenye nguvu ulikuwa ukivuma.[e] **19** Hata hivyo, walipokuwa wamevuta makasia karibu kilometa tano au sita, wakamwona Yesu akitembea juu ya bahari akiwa anaikaribia mashua; nao wakaogopa.[f] **20** Lakini akawaambia: "Ni mimi; msiogope!"[g]
21 Kwa hiyo walikuwa na nia ya kumchukua ndani ya mashua, na mara hiyo mashua ikawa kwenye nchi kavu walikokuwa wakijaribu kwenda.[h]

22 Siku iliyofuata umati waliokuwa wamesimama upande ule mwingine wa bahari wakaona kwamba hapakuwa na mashua hapo ila moja ndogo, na kwamba Yesu hakuwa ameingia ndani ya mashua pamoja na wanafunzi wake bali wanafunzi wake tu ndio waliokuwa wameondoka; **23** lakini mashua kutoka Tiberia zilifika karibu na mahali ambapo walikula mkate baada ya Bwana kushukuru. **24** Kwa hiyo umati walipoona kwamba Yesu hakuwa hapo wala wanafunzi wake, wakapanda mashua zao ndogo wakaja mpaka Kapernaumu kumtafuta[a] Yesu.

25 Kwa hiyo walipompata ng'ambo ya bahari wakamwambia: "Rabi,[b] ulifika hapa wakati gani?" **26** Yesu akawajibu na kusema: "Kwa kweli kabisa ninawaambia ninyi, Mnanitafuta, si kwa sababu mliona ishara, bali kwa sababu mlikula mikate mkashiba.[c] **27** Fanyeni kazi, si kwa ajili ya chakula ambacho huharibika,[d] bali kwa ajili ya chakula ambacho hudumu kufikia uzima wa milele,[e] ambacho Mwana wa binadamu atawapa ninyi; kwa maana juu yake huyo, Baba, naam Mungu, ametia muhuri wake wa kibali."[f]

28 Kwa hiyo wakamwambia: "Tutafanya nini ili tutende kazi za Mungu?" **29** Yesu akajibu, akawaambia: "Hii ndiyo kazi ya Mungu, kwamba mmwamini[g] yule ambaye Huyo alimtuma."[h]
30 Kwa hiyo wakamwambia: "Basi, wewe unafanya ishara[i] gani, ili tuione, tukuamini? Ni kazi gani ambayo unafanya? **31** Mababu zetu walikula mana[j] nyikani, kama vile ambavyo imeandikwa,

SURA 6
a Mt 14:20 Mk 6:43 Lu 9:17
b Kum 18:15 Kum 18:18 Isa 9:6 Lu 24:19 Mdo 3:22
c Mt 14:23 Mk 6:45 Yoh 17:16 Yoh 18:36 Yak 1:27 Yak 4:4
d Mt 14:22 Mk 6:47
e Mt 8:24 Mt 14:24 Mk 6:48
f Mt 14:26 Mk 6:49
g Mt 14:27 Mk 6:50
h Mt 14:34 Mk 6:51

Safu ya 2
a Mk 1:37
b Yoh 1:38
c Yoh 6:11
d Hab 3:17
e Yoh 4:14 Yoh 17:3 Ro 6:23
f Zb 22:8 Mt 3:17 Mdo 2:22 2Pe 1:17
g Mdo 16:31 1Yo 3:23
h Yoh 7:29 Yoh 8:42
i Mt 12:38 Mk 8:12 Yoh 2:18 1Ko 1:22
j Kut 16:15 Hes 11:7 Ne 9:15 Yoh 6:49 1Ko 10:3

'Aliwapa mkate kutoka mbinguni ili wale.'"[a] **32** Kwa sababu hiyo Yesu akawaambia: "Kwa kweli kabisa ninawaambia ninyi, Musa hakuwapa ninyi mkate kutoka mbinguni, lakini Baba yangu anawapa ninyi mkate wa kweli kutoka mbinguni.[b] **33** Kwa maana mkate wa Mungu ni yule ambaye hushuka kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima." **34** Kwa hiyo wakamwambia: "Bwana, utupe sikuzote mkate huo."[c]

35 Yesu akawaambia: "Mimi ndio mkate wa uzima. Yule ambaye huja kwangu hataona njaa hata kidogo, naye anayeniamini hatapata kiu kamwe.[d] **36** Lakini nimewaambia ninyi, hata mmeniona na bado hamwamini.[e] **37** Kila kitu anachonipa Baba kitakuja kwangu, naye anayekuja kwangu sitamfukuza kamwe;[f] **38** kwa sababu nimeshuka kutoka mbinguni[g] kufanya, si mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenituma.[h] **39** Haya ndiyo mapenzi yake aliyenituma, kwamba nisipoteze kitu chochote kati ya vyote ambavyo amenipa bali kwamba nikifufue[i] katika siku ya mwisho. **40** Kwa maana haya ndiyo mapenzi ya Baba yangu, kwamba kila mtu ambaye humtazama Mwana na kumwamini awe na uzima wa milele,[j] nami nitamfufua katika siku ya mwisho."[k]

41 Kwa hiyo Wayahudi wakaanza kumnung'unikia kwa sababu alisema: "Mimi ndio mkate ambao ulishuka kutoka mbinguni";[l] **42** nao wakaanza kusema:[a] "Je, huyu si Yesu mwana wa Yosefu,[b] ambaye baba na mama yake sisi tunawajua? Anawezaje sasa kusema, 'Mimi nimeshuka kutoka mbinguni'?" **43** Yesu akajibu, akawaambia: "Acheni kunung'unika kati yenu wenyewe. **44** Hakuna mtu anayeweza kuja kwangu isipokuwa Baba, aliyenituma, amvute;[c] nami nitamfufua siku ya mwisho.[d] **45** Imeandikwa katika Manabii, 'Na wote watafundishwa na Yehova.'[e] Kila mtu ambaye amesikia kutoka kwa Baba na ambaye amejifunza huja kwangu.[f] **46** Si kwamba mwanadamu yeyote amemwona Baba,[g] ila yule aliyetoka kwa Mungu; huyo amemwona Baba.[h] **47** Kwa kweli kabisa ninawaambia, Yule ambaye huamini ana uzima wa milele.[i]

48 "Mimi ndio mkate[j] wa uzima. **49** Mababu zenu walikula mana[k] nyikani na bado wakafa. **50** Huu ndio mkate ambao hushuka kutoka mbinguni, ili yeyote apate kuula na asife. **51** Mimi ndio mkate ulio hai ulioshuka kutoka mbinguni; yeyote akila mkate huu ataishi milele; na, kwa kweli, mkate ambao nitatoa ni mwili[l] wangu kwa ajili ya uzima wa ulimwengu."[m]

52 Kwa hiyo Wayahudi wakaanza kushindana, wakisema: "Mtu huyu anawezaje kutupa mwili wake tule?" **53** Basi Yesu akawaambia: "Kwa kweli kabisa ninawaambia, Ninyi msipoula mwili[n] wa Mwana wa binadamu na kunywa damu[o] yake, hamna uzima[p] ndani yenu we-

SURA 6
a Zb 78:24
Zb 105:40
b Yoh 3:16
c Yoh 4:15
d Yoh 4:14
Yoh 7:37
Ufu 22:17
e Yoh 6:64
f Mt 11:28
Yoh 17:6
g Yoh 3:13
Yoh 8:23
Yoh 8:42
h Mt 26:39
Yoh 5:30
i Yoh 5:28
Yoh 17:12
Ro 6:5
j Yoh 10:28
k Da 12:13
Yoh 11:24
Mdo 17:31
1Th 4:16
Ufu 20:12
l Yoh 6:33

Safu ya 2
a Mt 13:55
Mk 6:3
Lu 4:22
b Lu 3:23
c Yoh 6:65
2Th 2:13
d Yoh 11:24
e Isa 54:13
Yer 31:34
Mik 4:2
f 1Th 4:9
g Kut 33:20
h Mt 11:27
Lu 10:22
Yoh 1:18
i Yoh 3:16
j Yoh 6:33
k Yoh 6:31
l Yoh 1:14
1Yo 4:2
m Ebr 10:10
n Yoh 6:27
Yoh 6:33
o Mdo 20:28
Ro 3:25
p Ufu 20:4
Ufu 20:5

nyewe. **54** Yule ambaye hula
mwili wangu na kunywa damu
yangu ana uzima wa milele,
nami nitamfufua[a] katika siku ya
mwisho; **55** kwa maana mwi-
li wangu ni chakula cha kweli,
na damu yangu ni kinywaji cha
kweli. **56** Yule ambaye hula
mwili wangu na kunywa damu
yangu hukaa katika muunga-
no nami, na mimi katika mu-
ungano naye.[b] **57** Kama vile
Baba aliye hai[c] alivyonituma,
nami ninaishi kwa sababu ya
Baba, yule ambaye pia huni-
la mimi, hata huyo ataishi kwa
sababu yangu.[d] **58** Huu ndio
mkate ulioshuka kutoka mbi-
nguni. Si kama wakati maba-
bu zenu walipokula na bado
wakafa. Yule ambaye hula
mkate huu ataishi milele."[e]
59 Mambo haya aliyasema
alipokuwa akifundisha katika
kusanyiko la watu wote katika
Kapernaumu.

60 Kwa hiyo wengi kati ya
wanafunzi wake, waliposikia
hilo, wakasema: "Maneno hayo
yanashtua; ni nani ambaye ana-
weza kuyasikiliza?"[f] **61** La-
kini Yesu, akijua ndani yake
mwenyewe kwamba wanafu-
nzi wake walikuwa wakinu-
ng'unika juu ya hili, akawaa-
mbia: "Je, jambo hili linawa-
kwaza[g] ninyi? **62** Kwa hiyo,
namna gani ikiwa mtamwo-
na Mwana wa binadamu akipa-
nda kwenda alikokuwa mape-
ma?[h] **63** Roho ndiyo inayoto-
keza uzima;[i] mwili hauna faida
hata kidogo. Maneno ambayo
nimewaambia ni roho[j] na ni uzi-
ma.[k] **64** Lakini kuna wengi-
ne kati yenu ambao hawaami-
ni." Kwa maana tangu mwa-
nzo Yesu alijua ni nani wale
waliokuwa hawaamini na ni
nani angemsaliti.[a] **65** Kwa
hiyo akaendelea kusema: "Hii
ndiyo sababu nimewaambia ni-
nyi, Hakuna anayeweza kuja
kwangu isipokuwa aruhusiwe
na Baba."[b]

66 Kwa sababu ya hili wengi
kati ya wanafunzi wake wakae-
nda zao kwenye mambo yaliyo
nyuma[c] wakawa hawatembei
tena pamoja naye.[d] **67** Kwa
hiyo Yesu akawaambia wale
kumi na wawili: "Je, ninyi pia
mnataka kwenda?" **68** Simo-
ni Petro[e] akamjibu: "Bwana, tu-
taenda kwa nani?[f] Wewe una
maneno ya uzima wa milele;[g]
69 na sisi tumeamini na tume-
jua kwamba wewe ndiye Mta-
katifu wa Mungu."[h] **70** Yesu
akawajibu: "Niliwachagua ni-
nyi kumi na wawili,[i] sivyo? La-
kini mmoja wenu ni mchonge-
zi."[j] **71** Kwa kweli, alikuwa
akisema juu ya Yuda mwana wa
Simoni Iskariote; kwa maana
huyu alikuwa karibu kumsali-
ti,[k] ajapokuwa mmoja wa wale
kumi na wawili.

7 Basi baada ya mambo hayo
Yesu akaendelea kute-
mbea katika Galilaya, kwa ma-
ana hakutaka kutembea kati-
ka Yudea, kwa sababu Waya-
hudi walikuwa wakitafuta
kumuua.[l] **2** Hata hivyo, she-
rehe ya Wayahudi, ile shere-
he ya vibanda,[m] ilikuwa ka-
ribu. **3** Kwa hiyo ndugu[n]
zake wakamwambia: "Ondoka
hapa uende Yudea, ili wanafu-
nzi wako pia wapate kuona
kazi unazofanya. **4** Kwa ma-
ana hakuna mtu anayefanya
jambo lolote katika siri huku

SURA 6
a Yoh 6:40
1Ko 15:52
1Th 4:16
b Yoh 14:23
Yoh 15:4
1Yo 3:24
c Yer 10:10
Da 6:26
2Ko 3:3
1Th 1:9
d Yoh 5:26
1Ko 15:22
e Yoh 6:51
f Mt 11:6
Yoh 6:66
g Mt 13:21
h Yoh 3:13
Yoh 6:38
Yoh 8:23
Mdo 1:9
Efe 4:8
i 1Ko 15:45
2Ko 3:6
Ga 6:8
j 1Ko 2:13
k Kum 8:3
Zb 119:50
Mt 4:4
Flp 2:16

Safu ya 2
a Mt 9:4
Yoh 2:24
Yoh 13:11
b Yoh 6:44
c Lu 9:62
d Mt 11:6
Yoh 6:60
e Mt 16:16
Mk 8:29
f Ufu 14:4
g Yoh 6:63
Yoh 17:3
Mdo 5:20
h Mk 1:24
Lu 9:20
i Lu 6:13
Yoh 15:16
j Lu 22:3
Yoh 13:18
k Mt 26:14
Yoh 12:4

SURA 7
l Mk 9:30
Yoh 5:18
m Law 23:34
n Mt 12:46
Mk 6:3
Lu 8:19
Yoh 2:12
Mdo 1:14
Ga 1:19

yeye mwenyewe akitafuta ku-
julikana hadharani. Ikiwa
unafanya mambo hayo, jiony-
eshe mwenyewe kwa ulimwe-
ngu." **5** Kwa kweli, ndugu[a]
zake walikuwa hawamwami-
ni.[b] **6** Kwa hiyo Yesu akawaa-
mbia: "Wakati wangu unaofaa
haujafika bado,[c] lakini wakati
wenu unaofaa upo sikuzote.
7 Ulimwengu hauna sababu
ya kuwachukia ninyi, lakini
huo unanichukia mimi, kwa
sababu ninatoa ushahidi juu
yake kwamba kazi zake ni mbo-
vu.[d] **8** Pandeni mwende kwe-
nye sherehe; mimi bado sipandi
kwenda kwenye sherehe hiyo,
kwa sababu wakati wangu una-
ofaa[e] bado haujafika kikami-
li."[f] **9** Kwa hiyo baada ya ku-
waambia mambo haya, akabaki
Galilaya.

10 Lakini ndugu zake wali-
pokuwa wamepanda kwenda
kwenye sherehe, yeye mwenye-
we pia akapanda kwenda, si wa-
ziwazi bali kama katika siri.[g]
11 Kwa hiyo Wayahudi wakaan-
za kumtafuta[h] kwenye shere-
he na kusema: "Yuko wapi yule
mtu?" **12** Na umati ulikuwa
ukinong'onezana mambo me-
ngi juu yake.[i] Baadhi yao wa-
kawa wakisema: "Yeye ni
mtu mwema." Wengine waka-
wa wakisema: "Sivyo, bali yeye
anaupotosha umati." **13** Bila
shaka, hakuna aliyekuwa aki-
sema juu yake hadharani kwa
sababu ya kuwaogopa Waya-
hudi.[j]

14 Kufikia sasa sherehe ili-
pokuwa imefika katikati, Yesu
akapanda kuingia hekaluni na
kuanza kufundisha.[k] **15** Kwa
hiyo Wayahudi wakaanza ku-
staajabu, wakisema: "Mtu huyu
amepataje ujuzi wa maandi-
shi,[a] na yeye hajajifunza shu-
leni?"[b] **16** Yesu naye akawaji-
bu na kusema: "Yale ninayofu-
ndisha si yangu, bali ni yake
yeye aliyenituma.[c] **17** Ikiwa
yeyote anatamani kufanya ma-
penzi Yake, atajua kama fundi-
sho hilo limetoka kwa Mungu[d]
au kama ninasema mambo
ambayo nimetunga mimi mwe-
nyewe. **18** Yule ambaye hu-
sema mambo aliyotunga yeye
mwenyewe anatafuta utukufu
wake mwenyewe; bali yule ana-
yetafuta utukufu[e] wake aliye-
mtuma, huyo ni wa kweli, na
hakuna ukosefu wa uadilifu
ndani yake. **19** Musa aliwapa
ninyi Sheria,[f] sivyo? Lakini ha-
kuna hata mmoja kati yenu ana-
yetii Sheria. Kwa nini mnatafu-
ta kuniua?"[g] **20** Umati waka-
jibu: "Wewe una roho mwovu.[h]
Ni nani anayetaka kukuua?"
21 Yesu akajibu, akawaambia:
"Nilifanya tendo moja,[i] nanyi
nyote mnastaajabu. **22** Kwa
sababu hiyo Musa amewapa to-
hara[j]—si kwamba inatoka kwa
Musa, bali kwamba inatoka kwa
mababu[k]—nanyi mnatahiri mtu
siku ya sabato. **23** Ikiwa mtu
anatahiriwa siku ya sabato ili
sheria ya Musa isivunjwe, je,
mnanikasirikia kwa sababu ni-
limfanya mtu awe na afya nzu-
ri siku ya sabato?[l] **24** Acheni
kuhukumu kwa sura ya nje, bali
hukumuni kwa hukumu ya ua-
dilifu."[m]

25 Kwa hiyo baadhi ya
wakaaji wa Yerusalemu wa-
kaanza kusema: "Huyu ndi-
ye mtu ambaye wanatafuta ku-
muua,[n] sivyo? **26** Na bado,

SURA 7

a Mt 13:55
Lu 8:20
b Mk 3:21
c Yoh 2:4
Yoh 7:30
d Yoh 3:19
Yoh 15:19
e Mt 26:45
f Yoh 8:20
g Mt 10:16
h Yoh 11:56
i Mt 21:46
Lu 7:16
Yoh 6:14
Yoh 9:16
j Yoh 9:22
Yoh 12:42
Yoh 19:38
k Lu 19:47

Safu ya 2

a Lu 4:16
b Mt 13:54
Mk 6:2
Lu 2:47
Mdo 4:13
c Yoh 3:34
Yoh 8:28
Yoh 12:49
Yoh 14:10
Ufu 1:1
d Yoh 8:47
e Yoh 5:41
Yoh 8:50
f Kut 24:3
Kum 33:4
Mdo 7:38
Ga 3:19
g Mt 12:14
Mk 3:6
h Yoh 8:48
Yoh 10:20
i Yoh 5:16
j Law 12:3
k Mwa 17:10
Mwa 21:4
Ro 4:11
Flp 3:5
l Yoh 5:9
m Kum 1:16
Met 24:23
Isa 11:3
Mt 23:23
n Yoh 5:18

oneni! anasema hadharani,[a]
nao hawamwambii jambo lolote. Je, watawala wanajua kwa
hakika kwamba huyu ndiye
Kristo?[b] **27** Badala yake, sisi
tunajua mtu huyu ametoka
wapi;[c] lakini Kristo atakapokuja, hakuna atakayejua ametoka wapi."[d] **28** Kwa hiyo Yesu
akapaaza sauti alipokuwa akifundisha katika hekalu na kusema: "Ninyi mnanijua tena
mnajua nimetoka wapi.[e] Pia, sikuja kwa uamuzi wangu mwenyewe,[f] lakini yule aliyenituma ni halisi,[g] nanyi hammjui.[h]
29 Mimi ninamjua,[i] kwa sababu mimi ni mwakilishi kutoka kwake, na Yeye alinituma."[j]
30 Kwa hiyo wakaanza kutafuta kumkamata,[k] lakini hakuna aliyemkamata, kwa sababu saa[l] yake ilikuwa haijafika bado. **31** Bado, wengi kati
ya umati walimwamini;[m] nao
wakaanza kusema: "Kristo atakapofika, je, atafanya ishara[n]
zaidi ya zile ambazo mtu huyu
amefanya?"

32 Mafarisayo walisikia
umati wakinong'onezana mambo hayo juu yake, nao wakuu
wa makuhani na Mafarisayo
wakatuma maofisa wamkamate.[o] **33** Kwa hiyo Yesu akasema: "Nitaendelea kuwa pamoja nanyi muda kidogo zaidi kabla ya kwenda kwake aliyenituma.[p] **34** Mtanitafuta, lakini
hamtanipata,[q] na mahali nilipo hamwezi kuja."[r] **35** Kwa
hiyo Wayahudi wakasema kati
yao wenyewe: "Mtu huyu anakusudia kwenda wapi, hata
kwamba hatutampata? Je,
anakusudia kwenda kwa Wayahudi waliotawanyika[s] katikati

SURA 7

a Mt 26:55
Yoh 18:20
b Yoh 7:48
c Mt 13:55
d Mwa 49:10
Mik 5:2
Ebr 7:3
e Mk 6:3
Yoh 8:14
f Yoh 8:42
g Yoh 8:26
h Yoh 8:55
i Mt 11:27
Yoh 1:18
Yoh 10:15
j Ebr 3:1
k Mk 11:18
Lu 19:47
l Lu 22:53
Yoh 8:20
m Yoh 2:23
Yoh 8:30
Yoh 10:42
Yoh 11:45
n Mik 5:4
Yoh 11:47
o Yoh 11:57
p Yoh 13:33
Yoh 16:16
q Yoh 8:21
r Yoh 8:22
s Isa 11:12
Mdo 17:10
1Pe 1:1

Safu ya 2

a Law 23:36
b Isa 55:1
Yoh 4:14
Yoh 6:35
Ufu 22:17
c Kum 18:15
d Kut 17:6
Hes 20:8
Met 18:4
Yoh 4:14
1Ko 10:4
e Isa 44:3
Yoe 2:28
Yoh 16:7
Mdo 2:17
f Yoh 12:16
Yoh 13:32
1Ti 3:16
g Kum 18:18
Yoh 1:21
Yoh 6:14
Mdo 3:22
h Yoh 6:69
i Yoh 4:42
Yoh 7:52
j Yoh 1:46
k 2Nya 13:5
Zb 89:4
Zb 132:11
Yer 23:5
l Mik 5:2
Mt 2:5
Lu 2:4
m 1Sa 16:1
n Yoh 9:16
Yoh 10:19

ya Wagiriki na kuwafundisha Wagiriki? **36** Yanamaanisha
nini maneno hayo aliyosema
kwamba, 'Mtanitafuta, lakini
hamtanipata, na mahali nilipo
hamwezi kuja'?"

37 Basi siku ya mwisho, ile
siku kuu ya sherehe,[a] Yesu alikuwa amesimama, naye akapaaza sauti, akisema: "Ikiwa yeyote ana kiu,[b] acheni aje kwangu
na kunywa. **38** Yule ambaye
ananiamini,[c] kama vile Andiko
lilivyosema, 'Vijito vya maji yaliyo hai vitatiririka kutoka katika sehemu yake ya ndani kabisa.'"[d] **39** Hata hivyo, alisema hilo kuhusu ile roho ambayo
wale waliomwamini wangepokea hivi karibuni; kwa maana kufikia wakati huo roho[e]
haikuwapo, kwa sababu Yesu
hakuwa ametukuzwa[f] bado.
40 Kwa hiyo baadhi ya umati
ambao walisikia maneno hayo
wakaanza kusema: "Kwa hakika huyu ni Yule Nabii."[g]
41 Wengine walikuwa wakisema: "Huyu ndiye Kristo."[h] Lakini wengine walikuwa wakisema: "Je, kwa hakika Kristo[i] atakuja kutoka Galilaya?[j] **42** Je,
Andiko halijasema kwamba
Kristo anakuja kutoka kwa
uzao wa Daudi,[k] na kutoka Bethlehemu[l] kijiji ambako Daudi
alikaa?"[m] **43** Kwa hiyo mgawanyiko juu yake ukatokea
kati ya umati.[n] **44** Ingawa hivyo, baadhi yao walikuwa wakitafuta kumkamata, lakini hakuna aliyemkamata.

45 Kwa hiyo maofisa wakarudi kwa wakuu wa makuhani na Mafarisayo, na Mafarisayo wakawaambia: "Kwa
nini hamkumleta?" **46** Wale

maofisa wakajibu: "Mtu mwingine hajapata kamwe kusema kama huyu."[a] **47** Nao Mafarisayo wakajibu: "Je, ninyi pia mmepotoshwa? **48** Je, kuna hata mmoja wa watawala au wa Mafarisayo ambaye amemwamini?[b] **49** Lakini umati huu usiojua Sheria ni watu waliolaaniwa."[c] **50** Nikodemo, aliyekuwa amemwendea hapo kwanza, na aliyekuwa mmoja wao, akawaambia: **51** "Je, sheria yetu humhukumu mtu isipokuwa kwanza iwe imesikia[d] kutoka kwake na kujua analofanya?" **52** Wakajibu, wakamwambia: "Je, wewe pia umetoka Galilaya? Chunguza uone kwamba hakuna nabii[e] atakayeinuliwa kutoka Galilaya."*

8 **12** Kwa hiyo Yesu akawaambia tena, akisema: "Mimi ndiye nuru[f] ya ulimwengu. Yule anayenifuata hatatembea kamwe katika giza,[g] bali atakuwa na nuru ya uzima." **13** Kwa sababu hiyo Mafarisayo wakamwambia: "Wewe unatoa ushahidi juu yako mwenyewe; ushahidi wako si wa kweli." **14** Yesu akajibu, akawaambia: "Hata ikiwa ninatoa ushahidi juu yangu mwenyewe, ushahidi[a] wangu ni wa kweli, kwa sababu ninajua nilikotoka na ninakoenda.[b] Lakini ninyi hamjui nilitoka wapi na ninaenda wapi. **15** Ninyi mnahukumu kulingana na mwili;[c] mimi sihukumu mtu yeyote hata kidogo.[d] **16** Na bado ikiwa ninahukumu, hukumu yangu ni ya kweli, kwa sababu siko peke yangu, bali Baba aliyenituma yuko pamoja nami.[e] **17** Pia, katika Sheria yenu wenyewe imeandikwa, 'Ushahidi wa watu wawili ni wa kweli.'[f] **18** Mimi ninatoa ushahidi juu yangu mwenyewe, na Baba aliyenituma hutoa ushahidi juu yangu."[g] **19** Kwa hiyo wakaendelea kumwambia: "Yuko wapi Baba yako?" Yesu akajibu: "Ninyi hamnijui mimi wala Baba yangu.[h] Kama mngeni-

SURA 7
a Mwa 49:21; Mt 7:29; Lu 4:22; Lu 20:39
b Yoh 12:42; Mdo 6:7
c Ga 3:10
d Kum 1:16; Kum 17:8; Met 18:13
e Isa 9:1; Mt 4:15

SURA 8
f Isa 9:2; Isa 49:6; Mt 4:16; Yoh 1:5; Yoh 12:35
g Mik 3:6; Yoh 12:46; 1Pe 2:9; 1Yo 2:8

Safu ya 2
a Yoh 5:31
b Yoh 7:28; Yoh 13:3; Yoh 16:28
c 1Sa 16:7; Yoh 7:24
d Lu 12:14; Yoh 3:17
e Yoh 14:10; Yoh 16:32
f Kum 17:6; Kum 19:15; Mt 18:16; 2Ko 13:1; Ebr 10:28
g Yoh 5:37; 2Pe 1:17; 1Yo 5:9
h Yoh 16:3

---

* Hati Codex Sinaiticus, Codex Vaticanus, na Sinaitic Syriac codex huondoa mstari wa 53 mpaka sura ya 8, mstari wa 11, ambao husomwa (kukiwa na tofauti fulani-fulani katika maandishi mbalimbali na tafsiri za Kigiriki) kama ifuatavyo:

53 Kwa hiyo wakaenda kila mmoja nyumbani kwake.

8 Lakini Yesu akaenda kwenye Mlima wa Mizeituni. **2** Hata hivyo, wakati wa mapambazuko akajitokeza tena hekaluni, na watu wote wakaanza kumwendea, naye akaketi na kuanza kuwafundisha. **3** Basi waandishi na Mafarisayo wakamleta mwanamke aliyekuwa amepatikana akifanya uzinzi, na, baada ya kumsimamisha katikati yao, **4** wakamwambia: "Mwalimu, mwanamke huyu amepatikana akifanya uzinzi. **5** Katika Sheria Musa aliagiza kwamba tuwapige kwa mawe wanawake kama hawa. Kwa kweli, unasema nini?" **6** Bila shaka, walikuwa wakisema hilo ili kumjaribu, ili wawe na jambo fulani la kumshtakia. Lakini Yesu akainama, akaanza kuandika chini kwa kidole chake. **7** Walipozidi kumuuliza, akainuka na kuwaambia: "Yule kati yenu ambaye hana dhambi awe wa kwanza kumtupia jiwe." **8** Akainama tena na kuendelea kuandika chini. **9** Lakini wale waliosikia hilo wakaanza kuondoka wakienda, mmoja mmoja, kuanzia na wanaume wazee, naye akabaki peke yake, pamoja na mwanamke aliyekuwa katikati yao. **10** Yesu akainuka, akamwambia: "Mwanamke, wako wapi? Je, hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia?" **11** Yule mwanamke akasema: "Hakuna, bwana." Yesu akasema: "Wala mimi sikuhukumu kuwa na hatia. Ondoka uende zako; tangu sasa na kuendelea usiendelee kutenda dhambi tena."

jua mimi, mngemjua Baba yangu pia."[a] **20** Alisema maneno hayo katika chumba cha hazina[b] alipokuwa akifundisha katika hekalu. Lakini hakuna aliyemkamata,[c] kwa sababu saa[d] yake ilikuwa haijafika bado.

21 Kwa sababu hiyo akawaambia tena: "Ninaenda zangu, nanyi mtanitafuta,[e] na bado mtakufa katika dhambi yenu.[f] Ninakoenda hamwezi kuja." **22** Kwa hiyo Wayahudi wakaanza kusema: "Je, atajiua mwenyewe? Kwa sababu anasema, 'Ninakoenda hamwezi kuja.'"[g] **23** Kwa hiyo akaendelea kuwaambia: "Ninyi mnatoka kwenye makao ya chini; mimi ninatoka kwenye makao ya juu.[h] Ninyi mnatoka katika ulimwengu[i] huu; mimi sitoki katika ulimwengu huu.[j] **24** Kwa hiyo niliwaambia ninyi, Mtakufa katika dhambi zenu.[k] Kwa maana ikiwa hamwamini kwamba mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu."[l] **25** Kwa hiyo wakaanza kumwambia: "Wewe ni nani?" Yesu akawaambia: "Kwa nini hata ninasema nanyi? **26** Nina mambo mengi ya kusema juu yenu na kutoa hukumu juu ya mambo hayo. Kwa hakika, yule aliyenituma ni wa kweli, na mambo yale niliyoyasikia kutoka kwake ninayasema ulimwenguni."[m] **27** Hawakufahamu kwamba alikuwa akiwaambia juu ya Baba. **28** Kwa hiyo Yesu akasema: "Mara tu mkiisha kumwinua[n] Mwana wa binadamu,[o] ndipo mtakapojua kwamba mimi ndiye,[p] na kwamba sifanyi jambo lolote kwa uamuzi wangu mwenyewe;[a] bali kama vile Baba alivyonifundisha, ndivyo ninavyosema mambo haya.[b] **29** Na yule aliyenituma yuko pamoja nami; yeye hakuniacha peke yangu, kwa sababu sikuzote mimi hufanya mambo yanayompendeza."[c] **30** Alipokuwa akisema mambo haya, wengi walimwamini.[d]

31 Na kwa hiyo, Yesu akaendelea kuwaambia Wayahudi waliokuwa wamemwamini: "Mkikaa katika neno langu,[e] ninyi kwa kweli ni wanafunzi wangu, **32** nanyi mtaijua kweli,[f] nayo kweli itawaweka ninyi huru."[g] **33** Wakamjibu: "Sisi ni uzao wa Abrahamu[h] nasi hatujapata kamwe kuwa watumwa wa mtu yeyote.[i] Kwa nini basi unasema, 'Ninyi mtakuwa huru'?" **34** Yesu akawajibu: "Kwa kweli kabisa ninawaambia ninyi, Kila mtendaji wa dhambi ni mtumwa wa dhambi.[j] **35** Zaidi ya hayo, mtumwa hakai nyumbani milele; mwana hukaa milele.[k] **36** Kwa hiyo Mwana akiwaweka ninyi huru, mtakuwa huru kwelikweli.[l] **37** Ninajua kwamba ninyi ni uzao wa Abrahamu; lakini mnatafuta kuniua,[m] kwa sababu neno langu halifanyi maendeleo kati yenu.[n] **38** Mambo ambayo nimeyaona kwa Baba yangu[o] ninayasema;[p] na kwa hiyo, fanyeni mambo ambayo mmesikia kutoka kwa baba yenu." **39** Wakajibu, wakamwambia: "Baba yetu ni Abrahamu."[q] Yesu akawaambia: "Ikiwa ninyi ni watoto wa Abrahamu,[r] fanyeni kazi za Abrahamu. **40** Lakini sasa mnatafuta kuniua,

SURA 8

a Mt 11:27
Yoh 14:7
b Mk 12:41
c Yoh 7:30
d Yoh 7:8
e Yoh 7:34
Yoh 13:33
f Yoh 8:24
g Yoh 7:35
h Yoh 3:31
Yoh 16:28
Kol 3:1
i Yoh 15:19
Yoh 17:6
1Yo 4:5
j Yoh 18:36
k Eze 18:4
l Zb 51:5
Isa 58:1
m Yoh 7:28
Yoh 18:20
n Hes 21:9
Yoh 3:14
Yoh 12:32
Ga 3:13
o Da 7:13
Mt 26:64
p Mt 27:54

Safu ya 2

a Yoh 5:19
Yoh 5:30
b Yoh 3:11
c Met 8:13
Yoh 4:34
Yoh 14:10
Ebr 1:9
d Yoh 7:31
Yoh 10:42
Yoh 11:45
e Yoh 5:38
Yoh 15:7
f Yoh 17:17
Yoh 18:37
g Zb 119:45
Lu 4:18
Ro 6:14
Ro 6:22
Ebr 2:15
Yak 1:25
h Mt 3:9
i Law 25:42
j Met 5:22
Ro 6:6
Ro 6:16
Ro 7:14
2Pe 2:19
k Mwa 21:10
Mwa 25:6
Ga 4:30
l Ga 5:1
m Yoh 7:19
n Flp 3:16
o Yoh 5:19
p Yoh 14:10
q Mwa 26:4
Mt 3:9
Yoh 8:33
r Ro 2:28
Ro 9:8
Ga 3:7
Ga 3:29

mtu ambaye amewaambia kweli ambayo nilisikia kutoka kwa Mungu.[a] Abrahamu hakufanya hivyo.[b] **41** Ninyi mnafanya kazi za baba yenu." Wakamwambia: "Sisi hatukuzaliwa kutokana na uasherati; tuna Baba mmoja,[c] Mungu."

42 Yesu akawaambia: "Kama Mungu angekuwa ndiye Baba yenu, mngenipenda,[d] kwa maana nilitoka kwa Mungu nami nipo hapa.[e] Wala sikuja kwa uamuzi wangu mwenyewe hata kidogo, lakini Huyo alinituma.[f] **43** Kwa nini hamjui yale ninayosema? Kwa sababu hamwezi kusikiliza neno langu.[g] **44** Ninyi mmetoka kwa baba yenu Ibilisi,[h] nanyi mnataka kufanya tamaa za baba yenu.[i] Huyo alikuwa muuaji alipoanza,[j] naye hakusimama imara katika kweli, kwa sababu kweli haimo ndani yake. Anaposema uwongo, yeye husema kulingana na mwelekeo wake mwenyewe, kwa sababu yeye ni mwongo na ndiye baba ya uwongo.[k] **45** Kwa sababu mimi, kwa upande mwingine, ninawaambia ile kweli, hamniamini.[l] **46** Ni nani kati yenu anayenihukumu kuwa na hatia ya dhambi?[m] Ikiwa ninasema kweli, kwa nini hamniamini? **47** Yule anayetoka kwa Mungu husikiliza maneno ya Mungu.[n] Ndiyo sababu hamsikilizi, kwa sababu hamtoki kwa Mungu."[o]

48 Wayahudi wakajibu, wakamwambia: "Je, sisi hatusemi kweli kwamba, Wewe ni Msamaria[p] na una roho mwovu?"[q] **49** Yesu akajibu: "Mimi sina roho mwovu, lakini namheshimu Baba yangu,[r] nanyi mnanivunjia heshima. **50** Lakini mimi sijitafutii utukufu;[a] kuna Mmoja anayetafuta na anayehukumu.[b] **51** Kwa kweli kabisa ninawaambia, Yeyote akishika neno langu, hataona kifo kamwe."[c] **52** Wayahudi wakamwambia: "Sasa tunajua una roho mwovu.[d] Abrahamu alikufa,[e] pia manabii;[f] lakini wewe unasema, 'Yeyote akishika neno langu, hataonja[g] kifo kamwe.' **53** Je, wewe ni mkuu[h] kuliko Abrahamu baba yetu, ambaye alikufa? Pia, manabii walikufa.[i] Wewe unadai kuwa nani?" **54** Yesu akajibu: "Ikiwa mimi ninajitukuza mwenyewe, utukufu wangu si kitu. Baba yangu ndiye ambaye hunitukuza,[j] yule ambaye ninyi mnasema kwamba ni Mungu wenu; **55** na bado hamjamjua.[k] Lakini mimi ninamjua.[l] Na ikiwa ningesema simjui ningekuwa mwongo kama ninyi. Lakini mimi ninamjua, nami ninalishika neno lake.[m] **56** Baba yenu Abrahamu alishangilia sana katika tazamio la kuona siku yangu,[n] naye aliiona na kushangilia."[o] **57** Kwa hiyo Wayahudi wakamwambia: "Wewe hujafika umri wa miaka 50, na bado umemwona Abrahamu?" **58** Yesu akawaambia: "Kwa kweli ninawaambia ninyi, Kabla ya Abrahamu kuwako, mimi nimekuwako."[p] **59** Kwa hiyo wakaokota mawe wamtupie;[q] lakini Yesu akajificha na kutoka hekaluni.

9 Basi alipokuwa akipita alimwona mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa. **2** Na wanafunzi wake wakamuuliza: "Rabi,[r] ni nani aliyetenda dhambi,[s] ni mtu huyu au wazazi

SURA 8

a Yoh 8:26
b Ro 4:12
c Kum 32:6
Isa 63:16
Isa 64:8
Mal 1:6
Mal 2:10
d Yoh 16:27
1Yo 5:1
e Yoh 13:3
f Yoh 3:16
Yoh 5:19
Ga 4:4
g Ro 8:7
h Mt 4:1
Mt 13:39
1Pe 5:8
Ufu 12:9
i Mwa 3:15
Mt 12:34
Mdo 13:10
j 1Yo 3:8
k Mwa 3:4
2Ko 11:3
Ufu 12:9
l Lu 22:67
Yoh 6:64
m 2Ko 5:21
Ebr 4:15
Ebr 7:26
1Pe 2:22
1Yo 3:5
n Yoh 18:37
1Yo 4:6
o Yoh 10:26
p Yoh 4:9
q Mt 12:24
Yoh 7:20
Yoh 10:20
Yoh 15:18
r Mal 1:6

Safu ya 2

a Yoh 5:41
Yoh 7:18
b Mwa 18:25
Zb 26:1
Isa 33:22
Mdo 17:31
Ro 3:6
c Yoh 5:24
Yoh 11:26
1Ko 15:54
Ufu 20:6
d Yoh 10:20
e Mwa 25:8
f Zek 1:5
Mdo 2:29
Ebr 11:13
g Mt 16:28
h Yoh 4:12
i Mt 23:29
j Yoh 5:41
Yoh 13:32
Mdo 3:13
k Yoh 7:28
l Yoh 7:29
m Mt 17:5
n Lu 10:24
o Mt 13:17
Ebr 11:13
1Pe 1:11
p Met 8:22
Yoh 17:5
Flp 2:6
Kol 1:17
1Yo 2:13
q Yoh 10:31
Yoh 11:8

SURA 9

r Yoh 1:38
s Lu 13:2

wake,[a] hata kwamba akazaliwa kipofu?" **3** Yesu akajibu: "Mtu huyu hakutenda dhambi wala wazazi wake, bali ilikuwa hivyo ili kazi za Mungu zipate kufunuliwa katika kisa chake.[b] **4** Lazima tufanye kazi zake aliyenituma kukiwa mchana bado;[c] usiku[d] unakuja wakati ambapo hakuna mtu anayeweza kufanya kazi. **5** Maadamu nimo ulimwenguni, mimi ndiye nuru[e] ya ulimwengu." **6** Baada ya kusema hayo, akatema mate chini akafanyiza udongo kwa mate hayo, akauweka udongo wake juu ya macho ya mtu huyo[f] **7** na kumwambia: "Nenda ukanawe[g] katika dimbwi la Siloamu"[h] (linalotafsiriwa 'Aliyetumwa'). Na kwa hiyo akaenda na kunawa,[i] akarudi akiwa anaona.[j]

8 Kwa hiyo majirani na wale ambao hapo zamani walikuwa wakimwona akiombaomba wakaanza kusema: "Je, huyu siye yule mtu aliyekuwa akiketi na kuombaomba?"[k] **9** Baadhi yao wakawa wakisema: "Huyu ndiye." Wengine wakawa wakisema: "Sivyo hata kidogo, lakini anafanana na yeye." Mtu huyo akawa akisema: "Mimi ndiye." **10** Kwa hiyo wakaanza kumwambia: "Basi, macho yako yalifunguliwaje?"[l] **11** Akajibu: "Mtu anayeitwa Yesu alifanyiza udongo akaupaka juu ya macho yangu na kuniambia, 'Nenda mpaka Siloamu[m] ukanawe.' Kwa hiyo nikaenda, nikanawa na kupata kuona." **12** Ndipo wakamwambia: "Yuko wapi mtu huyo?" Akasema: "Sijui."

13 Wakampeleka kwa Mafarisayo mtu huyo aliyekuwa kipofu hapo zamani. **14** Ikawa kwamba siku ambayo Yesu aliufanyiza udongo na kuyafungua macho[a] yake ilikuwa siku ya Sabato.[b] **15** Kwa hiyo, wakati huo Mafarisayo pia wakazidi kumuuliza jinsi alivyopata kuona.[c] Akawaambia: "Aliuweka udongo juu ya macho yangu, nami nikanawa na ninaona." **16** Basi baadhi ya Mafarisayo wakaanza kusema: "Huyu si mtu anayetoka kwa Mungu, kwa sababu haishiki Sabato."[d] Wengine wakaanza kusema: "Mtu aliye mtenda-dhambi anawezaje kufanya ishara[e] kama hizo?" Basi kukawa na mgawanyiko[f] kati yao. **17** Kwa sababu hiyo, wakamwambia tena kipofu yule: "Wewe unasema nini juu yake, kwa kuwa aliyafungua macho yako?" Mtu yule akasema: "Yeye ni nabii."[g]

18 Hata hivyo, Wayahudi hawakuamini kumhusu yeye kwamba alikuwa kipofu na alikuwa amepata kuona, mpaka walipowaita wazazi wa mtu aliyepata kuona. **19** Nao wakawauliza: "Je, huyu ni mwana wenu ambaye mnasema alizaliwa akiwa kipofu? Basi, imekuwaje kwamba anaona sasa?" **20** Ndipo wazazi wake wakajibu, wakasema: "Sisi tunajua kwamba huyu ni mwana wetu na kwamba alizaliwa akiwa kipofu. **21** Lakini jinsi anavyoweza kuona sasa hatujui, wala hatujui ni nani aliyemfungua macho yake. Muulizeni yeye. Ana umri wa kutosha. Lazima ajisemee mwenyewe." **22** Wazazi wake walisema mambo hayo kwa sababu walikuwa wakiwaogopa[h] Wayahudi,

SURA 9

a Kut 20:5
Eze 18:19

b Mt 11:5
Yoh 11:4

c Yoh 4:34
Yoh 11:9

d Ayu 10:21
Mhu 9:10

e Isa 49:6
Isa 61:1
Yoh 1:5
Yoh 8:12

f Mk 8:23

g 2Fa 5:10

h 2Fa 20:20
2Nya 32:30

i 2Fa 5:14

j Isa 42:7

k Mdo 3:10

l Yoh 9:15

m Yoh 9:7

Safu ya 2

a Yoh 9:6

b Lu 13:14
Yoh 5:9

c Yoh 9:10

d Kut 20:10

e Yoh 3:2

f Lu 12:51
Yoh 7:12
Yoh 7:43
Yoh 10:19

g Kum 18:22
Yoh 4:19

h Met 29:25
Yoh 7:13
Yoh 19:38
Yoh 20:19

kwa maana Wayahudi walikuwa tayari wamefikia mapatano kwamba, ikiwa yeyote
angemkiri kuwa ndiye Kristo,
angefukuzwa katika sinagogi.[a]
23 Ndiyo sababu wazazi wake
walisema: "Ana umri wa kutosha. Muulizeni yeye."

24 Kwa hiyo wakamwita
mara ya pili mtu aliyekuwa
kipofu na kumwambia: "Mpe
Mungu utukufu;[b] sisi tunajua kwamba mtu huyu ni mtenda-dhambi." **25** Naye akajibu: "Kama yeye ni mtenda-dhambi mimi sijui. Mimi ninajua jambo moja, kwamba, ingawa nilikuwa kipofu, sasa ninaona."
26 Kwa hiyo wakamwambia:
"Alikufanyia nini? Aliyafunguaje macho yako?" **27** Akawajibu: "Tayari nimewaambia, na
bado hamkusikiliza. Kwa nini
mnataka kusikia tena? Je, ninyi pia mnataka kuwa wanafunzi wake?" **28** Ndipo wakamtukana na kusema: "Wewe ni
mwanafunzi wa mtu huyo, lakini sisi ni wanafunzi wa Musa.
29 Sisi tunajua kwamba Mungu amesema na Musa;[c] lakini mtu huyo, sisi hatujui anakotoka."[d] **30** Mtu yule akajibu, akawaambia: "Hakika hili
ni jambo la kustaajabisha,[e]
kwamba hamjui anakotoka,
naye aliyafungua macho yangu. **31** Tunajua kwamba
Mungu hawasikilizi watenda-dhambi,[f] bali ikiwa mtu yeyote anamwogopa Mungu na anafanya mapenzi yake, yeye
humsikiliza.[g] **32** Kutoka zamani za kale haijasikiwa kamwe kwamba mtu yeyote alifungua macho ya mtu aliyezaliwa akiwa kipofu. **33** Kama
mtu huyu hangekuwa ametoka kwa Mungu,[a] hangeweza
kufanya lolote." **34** Wakajibu, wakamwambia: "Wewe ulizaliwa katika dhambi,[b] na bado
je, wewe unatufundisha sisi?"
Nao wakamfukuza![c]

35 Yesu akasikia kwamba
walikuwa wamemfukuza, na,
alipompata, akasema: "Je, unamwamini Mwana[d] wa binadamu?" **36** Mtu huyo akajibu:
"Na huyo ni nani, bwana, ili
nipate kumwamini?" **37** Yesu
akamwambia: "Wewe umemwona na, mbali na hilo, yule anayesema na wewe ndiye huyo."[e]
38 Ndipo akasema: "Ninamwamini, Bwana." Naye akamsujudia.[f] **39** Na Yesu akasema:
"Kwa ajili ya hukumu[g] hii mimi
nilikuja katika ulimwengu huu:
ili wale ambao hawaoni[h] wapate
kuona na wale wanaoona wapate kuwa vipofu."[i] **40** Wale wa
Mafarisayo waliokuwa pamoja
naye wakasikia mambo hayo,
nao wakamwambia: "Je, sisi pia
ni vipofu?"[j] **41** Yesu akawaambia: "Kama mngekuwa vipofu, hamngekuwa na dhambi.
Lakini sasa mnasema, 'Tunaona.'[k] Dhambi[l] yenu inabaki."

10 "Kwa kweli ninawaambia ninyi, Yule asiyeingia katika zizi la kondoo kupitia mlango[m] bali hupandia mahali pengine, huyo ni mwizi
na mporaji.[n] **2** Lakini yule
anayeingia kupitia mlango[o]
ndiye mchungaji[p] wa kondoo.[q]
3 Mtunza-mlango[r] humfungulia huyo, nao kondoo[s] huisikiliza sauti yake, naye huwaita kondoo zake mwenyewe kwa
jina na kuwatoa nje. **4** Baada ya kuwatoa nje wote walio wake mwenyewe, yeye hue-

SURA 9
a Yoh 12:42
Yoh 16:2
b Yos 7:19
c Zb 103:7
d Yoh 8:14
e Yoh 3:10
f Zb 66:18
Met 28:9
Isa 1:15
Eze 8:18
Mik 3:4
Zek 7:13
g Zb 34:15
Met 15:29
Mdo 10:35

Safu ya 2
a Yoh 3:2
Yoh 5:36
b Yoh 9:2
c Yoh 9:22
Yoh 16:2
d 1Yo 5:13
e Yoh 4:26
f 1Sa 25:23
Mt 8:2
Mt 9:18
g Yoh 12:47
h Lu 4:18
Yoh 12:46
i Isa 29:14
Mt 11:25
Mt 13:13
Yoh 3:19
Mdo 28:26
Ro 1:28
2Pe 1:9
j Mt 15:14
Ro 2:19
Ufu 3:17
k Met 26:12
2Ko 4:4
l Yoh 15:22

SURA 10
m Yoh 10:7
n Mt 7:15
o Yoh 10:9
p Mt 26:31
Yoh 10:11
q Mk 14:27
Lu 12:32
r Mal 3:1
Lu 1:17
Yoh 3:28
s Yoh 10:27

nda mbele yao, nao kondoo hu-
mfuata,[a] kwa sababu wanaijua
sauti yake.[b] **5** Hawatamfua-
ta mgeni kamwe bali watamki-
mbia,[c] kwa sababu hawaijui sa-
uti ya wageni."[d] **6** Yesu ali-
waambia mfano huo; lakini ha-
wakujua mambo aliyowaambia
yalimaanisha nini.[e]

7 Kwa hiyo Yesu akasema
tena: "Kwa kweli ninawaambia
ninyi, Mimi ndiye mlango[f] wa
kondoo. **8** Wale wote ambao
wamekuja badala yangu ni wezi
na waporaji;[g] lakini kondoo ha-
wakuwasikiliza.[h] **9** Mimi ndi-
ye mlango;[i] yeyote yule anaye-
ingia kupitia kwangu ataoko-
lewa, naye ataingia na kutoka
na kupata malisho.[j] **10** Mwi-
zi[k] haji isipokuwa aje kuiba na
kuua na kuharibu.[l] Mimi nime-
kuja ili wapate kuwa na uzima
na wapate kuwa nao kwa wi-
ngi. **11** Mimi ndiye mchunga-
ji[m] mwema; mchungaji mwe-
ma huitoa nafsi yake kwa aji-
li ya kondoo.[n] **12** Mtu aliye-
kodiwa,[o] ambaye si mchungaji
na ambaye kondoo si wake, hu-
mwona mbwa-mwitu akija
naye huwaacha kondoo na ku-
kimbia—naye mbwa-mwitu hu-
wanyakua na kuwatawanya[p]—
13 kwa sababu huyo ni mtu
aliyekodiwa[q] naye hawajali ko-
ndoo.[r] **14** Mimi ndiye mchu-
ngaji mwema, nami ninawajua
kondoo[s] wangu na kondoo wa-
ngu wananijua,[t] **15** kama vile
Baba anavyonijua mimi nami
ninamjua Baba;[u] nami ninai-
toa nafsi yangu kwa ajili ya ko-
ndoo.[v]

16 "Nami nina kondoo we-
ngine,[w] ambao si wa zizi hili;[x]
hao pia nitawaleta, nao wata-
isikiliza sauti yangu,[a] nao wa-
takuwa kundi moja, mchunga-
ji mmoja.[b] **17** Ndiyo sababu
Baba ananipenda,[c] kwa sababu
ninaitoa nafsi yangu,[d] ili nipa-
te kuipokea tena. **18** Hakuna
mtu ambaye ameichukua ku-
toka kwangu, bali ninaitoa
kwa uamuzi wangu mwenye-
we. Nina mamlaka ya kuitoa,
nami nina mamlaka ya kui-
pokea tena.[e] Amri[f] kuhusu hili
niliipokea kutoka kwa Baba
yangu."

19 Tena mgawanyiko[g] ukato-
kea kati ya Wayahudi kwa saba-
bu ya maneno hayo. **20** Wengi
wao walikuwa wakisema: "Ana
roho mwovu[h] naye ana wa-
zimu. Kwa nini mnamsikiliza?"
21 Wengine wakawa wakisema:
"Haya si maneno ya mtu mwe-
nye roho mwovu. Je, roho mwo-
vu anaweza kufungua macho ya
vipofu?"

22 Wakati huo kulikuwa na
sherehe ya wakfu Yerusalemu.
Ulikuwa wakati wa majira ya
baridi kali, **23** na Yesu aliku-
wa akitembea hekaluni kati-
ka eneo lenye mistari ya ngu-
zo za Sulemani.[i] **24** Kwa hiyo
Wayahudi wakamzunguka na
kuanza kumwambia: "Utae-
ndelea kuzihangaisha nafsi
zetu mpaka wakati gani? Ikiwa
wewe ndiye Kristo,[j] tuambie
waziwazi."[k] **25** Yesu akawajibu:
"Niliwaambia, na bado ha-
mwamini. Kazi ninazotenda
katika jina la Baba yangu, hizo
zinatoa ushahidi juu yangu.[l]
26 Lakini hamwamini, kwa
sababu ninyi hamko kati ya
kondoo wangu.[m] **27** Kondoo[n]
wangu huisikiliza sauti yangu,
nami ninawajua, nao wananifu-
ata.[o] **28** Nami ninawapa hao

SURA 10

a Mt 4:20
Mt 9:9
Ufu 14:4
b Ufu 3:20
c Ufu 2:2
d Ga 1:8
Kol 2:8
e Yoh 16:25
f Yoh 14:6
g Yer 23:1
Eze 34:2
h Mdo 5:36
i Efe 2:18
j Yoh 21:17
k Ayu 24:14
Mt 7:15
l Mdo 20:29
2Pe 2:1
m Eze 34:23
Mt 9:36
n 1Sa 17:35
Isa 53:7
Ebr 13:20
o Ayu 7:2
Zek 11:16
p Mdo 20:29
q 1Pe 5:2
r Mk 12:40
s Yoh 10:27
t 1Yo 5:20
u Mt 11:27
v Mt 20:28
Yoh 15:13
1Yo 3:16
w Zb 45:14
Mt 25:33
Ufu 7:9
x Lu 12:32
Yoh 10:1

Safu ya 2

a Mwa 49:10
b Eze 34:23
Eze 37:24
1Pe 5:4
c Yoh 17:23
d Isa 53:12
Flp 2:8
Ebr 2:9
Ebr 12:2
e Yoh 2:19
Mdo 2:24
f Yoh 14:31
g Lu 12:51
Yoh 7:12
Yoh 9:16
h Mt 11:18
Mk 3:30
Lu 7:33
i Mdo 3:11
Mdo 5:12
j Mt 26:63
k Mk 8:30
l Yoh 3:2
Yoh 5:36
Yoh 10:38
Yoh 14:10
Mdo 2:22
m Yoh 6:64
Yoh 8:47
1Yo 4:6
n Lu 15:6
Yoh 10:3
o Mt 4:20
Mt 9:9
Ufu 14:4

uzima wa milele,[a] nao hawataharibiwa kamwe,[b] wala hakuna atakayewanyakua kutoka
mkononi mwangu.[c] **29** Kile
ambacho Baba[d] yangu amenipa
ni kikubwa zaidi kuliko vingine
vyote,[e] na hakuna anayeweza
kuwanyakua kutoka mkononi
mwa Baba.[f] **30** Mimi na Baba
ni kitu kimoja."[g]

31 Wayahudi wakaokota mawe
tena ili wampige.[h] **32** Yesu aka-
wajibu: "Niliwaonyesha kazi
nyingi nzuri kutoka kwa Baba.
Kati ya kazi hizo mnataka ku-
nipiga kwa mawe kwa sababu
ya kazi gani?" **33** Wayahu-
di wakamjibu: "Tunakupiga
kwa mawe, si kwa sababu ya
kazi njema, bali kwa sababu ya
kukufuru,[i] naam, kwa sababu,
ijapokuwa wewe ni mwanada-
mu, unajifanya kuwa mungu."[j]
34 Yesu akawajibu: "Je, haiku-
andikwa katika Sheria yenu,[k]
'Mimi nilisema: "Ninyi ni miu-
ngu"'?[l] **35** Ikiwa aliwaita 'mi-
ungu'[m] wale ambao neno la Mu-
ngu lilikuja dhidi yao, na bado
Andiko haliwezi kubatilishwa,[n]
36 je, mnaniambia mimi amba-
ye Baba alinitakasa na kunitu-
ma ulimwenguni, 'Unakufuru,'
kwa sababu nilisema, Mimi ni
Mwana wa Mungu?[o] **37** Ikiwa
mimi sitendi kazi[p] za Baba, msi-
niamini. **38** Lakini ikiwa ni-
nazitenda, hata ingawa hamni-
amini, iweni na imani katika
kazi hizo,[q] ili mjue na kuendelea
kujua kwamba Baba yuko kati-
ka muungano pamoja na mimi,
nami niko katika muungano
pamoja na Baba."[r] **39** Kwa
hiyo wakajaribu tena kumka-
mata;[s] lakini akaondoka miko-
noni mwao.[t]

SURA 10
a Yoh 5:24
Yoh 17:2
b Yoh 6:37
c Yoh 18:9
d Yoh 14:28
e Yoh 17:2
f Yoh 17:24
1Pe 1:5
g Yoh 10:38
Yoh 17:11
Yoh 17:21
h Yoh 8:59
i Law 24:16
Mt 9:3
Mt 26:65
j Yoh 5:18
Flp 2:6
k Yoh 15:25
l Zb 82:6
1Ko 8:5
m Zb 82:1
n Mt 5:17
Lu 16:17
o Lu 1:35
Yoh 5:18
p Yoh 5:36
q Yoh 14:10
r Yoh 17:21
s Yoh 7:30
t Lu 4:30

Safu ya 2
a Yoh 1:28
b Yoh 1:29
Yoh 3:30
c Yoh 8:30
Yoh 11:45

SURA 11
d Lu 10:38
e Mt 26:7
Mk 14:3
Yoh 12:3
f Lu 7:38
g Yoh 11:36
h Yoh 9:3
i Yoh 1:38
j Yoh 8:59
Yoh 10:31

40 Kwa hiyo akaenda tena
ng'ambo ya Yordani mpaka ma-
hali ambako Yohana alikuwa
akibatizia[a] hapo kwanza, naye
akakaa huko. **41** Na watu we-
ngi wakamjia, nao wakaanza
kusema: "Yohana, kwa kwe-
li, hakufanya hata ishara moja,
lakini mambo mengi ambayo
Yohana alisema juu ya mtu
huyu, yote yalikuwa ya kwe-
li."[b] **42** Na wengi wakamwa-
mini huko.[c]

11 Basi kulikuwa na mtu
fulani mgonjwa, Lazaro wa Bethania, wa kijiji cha Maria na cha Martha[d] dada yake. **2** Kwa kweli, Maria aliyempaka Bwana mafuta yenye marashi[e] na kufuta miguu yake ili kuikausha kwa nywele zake,[f] ndiye ambaye Lazaro ndugu yake alikuwa mgonjwa. **3** Kwa hiyo dada zake walipeleka neno kwake, wakisema: "Bwana, ona! yule unayempenda[g] ni mgonjwa." **4** Lakini Yesu aliposikia hilo akasema: "Lengo la ugonjwa huu si kifo, bali ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu,[h] ili Mwana wa Mungu atukuzwe kupitia huo."

5 Basi Yesu alimpenda Martha na dada yake na Lazaro. **6** Hata hivyo, aliposikia kwamba alikuwa mgonjwa, ndipo kwa kweli akakaa siku mbili mahali alipokuwa. **7** Kisha baada ya hayo, akawaambia wanafunzi: "Twendeni Yudea tena." **8** Wanafunzi wakamwambia: "Rabi,[i] juzijuzi tu Wayudea walikuwa wakitafuta kukupiga kwa mawe,[j] na je, unaenda huko tena?" **9** Yesu akajibu: "Kuna saa kumi na mbili za nuru ya mchana, si-

vyo? Ikiwa yeyote anatembea
katika nuru ya mchana[a] hagongi kitu chochote, kwa sababu anaona nuru ya ulimwengu
huu. **10** Lakini ikiwa yeyote anatembea usiku,[b] yeye hugonga kitu fulani, kwa sababu
nuru haimo ndani yake."

11 Alisema hayo, kisha akawaambia: "Lazaro rafiki yetu
anapumzika, lakini ninafunga safari kwenda huko ili kumwamsha kutoka usingizini."[c]
12 Kwa hiyo wanafunzi wakamwambia: "Bwana, ikiwa anapumzika, atapona." **13** Hata
hivyo, Yesu alikuwa amesema juu ya kifo chake. Lakini walifikiri alikuwa akisema juu
ya kupumzika katika usingizi. **14** Kwa hiyo, wakati huo, Yesu akawaambia waziwazi:
"Lazaro amekufa,[d] **15** nami ninashangilia kwa sababu yenu kwamba sikuwa huko, kusudi
ninyi mwamini. Lakini twendeni kwake." **16** Kwa hiyo Tomasi, aliyeitwa Pacha, akawaambia wanafunzi wenzake:
"Acheni twende pia, ili tukafe pamoja naye."[e]

17 Kwa hiyo Yesu alipofika, alikuta tayari amekwisha
kuwa ndani ya kaburi siku nne.[f] **18** Basi Bethania ilikuwa karibu na Yerusalemu umbali wa
karibu kilometa tatu. **19** Basi wengi kati ya Wayahudi walikuwa wamekuja kwa Martha
na Maria ili wawafariji[g] kuhusu ndugu yao. **20** Kwa hiyo Martha, aliposikia kwamba
Yesu anakuja, alienda kukutana naye; lakini Maria[h] akaendelea kuketi nyumbani. **21** Kwa
hiyo Martha akamwambia Yesu: "Bwana, kama ungekuwa
hapa ndugu yangu hangekufa.[a] **22** Hata hivyo sasa ninajua
kwamba mambo mengi kadiri unayomwomba Mungu,[b] Mungu atakupa." **23** Yesu akamwambia: "Ndugu yako atafufuka."[c] **24** Martha akamwambia: "Ninajua atafufuka katika ufufuo[d] siku ya mwisho."
25 Yesu akamwambia: "Mimi ndiye ufufuo na uzima.[e] Yule anayeniamini, hata akifa, atarudi kwenye uzima;[f] **26** na
kila mtu aliye hai na ananiamini hatakufa kamwe.[g] Je, unaamini hilo?" **27** Akamwambia: "Ndiyo, Bwana; nimeamini kwamba wewe ndiye Kristo
Mwana wa Mungu, Yule anayekuja ulimwenguni."[h] **28** Na alipokuwa amesema hilo, akaenda zake na kumwita Maria
dada yake, akisema kwa siri: "Mwalimu[i] yupo naye anakuita." **29** Aliposikia hilo, akasimama upesi, akamwendea.

30 Kwa kweli, Yesu alikuwa hajaingia kijijini, lakini bado
alikuwa mahali ambapo Martha alikutana naye. **31** Kwa hiyo Wayahudi waliokuwa pamoja naye nyumbani[j] na waliokuwa wakimfariji, walipomwona Maria akisimama upesi na
kuondoka aende, wakamfuata, wakidhani kwamba alikuwa akienda kwenye kaburi[k] ili
kulilia huko. **32** Na kwa hiyo Maria, alipofika mahali ambapo Yesu alikuwa na kumwona,
akajiangusha miguuni pake, akamwambia: "Bwana, kama ungekuwa hapa, ndugu yangu
hangekufa."[l] **33** Kwa hiyo, Yesu alipomwona akilia na Wayahudi waliokuja pamoja naye
wakilia, akaugua rohoni na

SURA 11

a Yoh 9:4
b Isa 5:20
Yoh 12:35
1Yo 2:11
c Zb 13:3
Mt 9:24
Mdo 7:60
1Ko 15:6
1Ko 15:51
d Mhu 9:5
e Yoh 11:8
f Mt 8:28
Yoh 5:28
g 1Nya 7:22
Ayu 2:11
h Lu 10:39

Safu ya 2

a Yoh 11:32
b Yoh 9:31
c 1Th 4:14
d Isa 26:19
Da 12:2
Yoh 5:29
Mdo 24:15
Ebr 11:35
Ufu 20:12
e Yoh 1:4
Yoh 14:6
Kol 3:4
1Yo 1:2
Ufu 1:18
f Yoh 5:24
g Yoh 8:51
h Mal 3:1
Yoh 4:42
Yoh 6:14
i Mt 23:8
Yoh 13:13
j Yoh 11:19
k Yoh 11:17
l Yoh 11:21

kutaabika;[a] **34** naye akasema: "Mmemlaza wapi?" Wakamwambia: "Bwana, njoo uone."
35 Yesu akatokwa na machozi.[b] **36** Kwa hiyo Wayahudi wakaanza kusema: "Ona, jinsi alivyokuwa akimpenda!"[c]
37 Lakini baadhi yao wakasema: "Je, mtu huyu aliyefungua macho[d] ya mtu aliye kipofu hakuweza kumzuia huyu asife?"

38 Kwa hiyo Yesu, baada ya kuugua tena ndani yake, akaja kwenye lile kaburi.[e] Kwa kweli, lilikuwa pango, na jiwe[f] lilikuwa limelilalia. **39** Yesu akasema: "Liondoeni jiwe."[g] Martha, dada ya yule aliyekufa, akamwambia: "Bwana, kufikia sasa lazima awe ananuka, kwa maana ni siku nne." **40** Yesu akamwambia: "Je, sikukuambia kwamba ukiamini utauona utukufu wa Mungu?"[h] **41** Kwa hiyo wakaliondoa jiwe. Basi Yesu akainua macho yake kuelekea mbinguni[i] na kusema: "Baba, ninakushukuru kwamba umenisikia.[j] **42** Kweli, nilijua kwamba sikuzote wewe hunisikia; lakini kwa sababu ya umati[k] waliosimama kunizunguka nilisema, ili wapate kuamini kwamba wewe ulinituma."[l] **43** Na alipokuwa amekwisha kusema hayo, akaita kwa sauti kubwa: "Lazaro, njoo huku nje!"[m]
44 Huyo mtu aliyekuwa mfu akatoka miguu na mikono yake ikiwa imefungwa vitambaa,[n] na uso wake ulikuwa umefungwa-fungwa kwa kitambaa. Yesu akawaambia: "Mfungueni, mmwache aende."

45 Kwa hiyo wengi kati ya Wayahudi waliokuwa wamekuja kwa Maria na walioona lile alilofanya, wakamwamini;[a]
46 lakini baadhi yao wakaenda zao kwa Mafarisayo na kuwaambia mambo aliyoyafanya Yesu.[b] **47** Kwa sababu hiyo wakuu wa makuhani na Mafarisayo wakaikusanya pamoja Sanhedrini[c] na kuanza kusema: "Tufanye nini, kwa sababu mtu huyu anafanya ishara nyingi?[d] **48** Tukimwacha hivyo, hao wote watamwamini,[e] na Waroma[f] watakuja na kuondolea mbali mahali[g] petu na taifa letu pia." **49** Lakini mtu fulani kati yao, Kayafa, aliyekuwa kuhani mkuu mwaka huo,[h] akawaambia: "Ninyi hamjui lolote kamwe, **50** nanyi hamwoni kwamba ni kwa faida yenu mtu mmoja afe[i] kwa ajili ya watu kuliko taifa lote liangamizwe."[j] **51** Ingawa hivyo, hilo hakulisema kwa kujitungia mwenyewe; lakini kwa sababu alikuwa kuhani mkuu mwaka huo, alitoa unabii kwamba Yesu alikusudiwa kufa kwa ajili ya taifa, **52** na si kwa ajili ya taifa hilo tu, bali ili watoto wa Mungu waliotawanyika[k] huku na huku yeye apate pia kuwakusanya pamoja kuwa mmoja.[l] **53** Kwa hiyo tangu siku hiyo na kuendelea wakakata shauri kumuua.[m]

54 Kwa sababu hiyo Yesu hakutembea tena huku na huku hadharani[n] kati ya Wayahudi,[o] bali aliondoka huko mpaka nchi iliyo karibu na nyika, akaingia katika jiji linaloitwa Efraimu,[p] na humo akakaa pamoja na wanafunzi. **55** Sasa pasaka[q] ya Wayahudi ilikuwa karibu, na watu wengi walipanda kutoka nchi

SURA 11

a Yoh 13:21
b Lu 19:41
Ro 12:15
Ebr 4:15
c Yoh 11:3
d Yoh 9:6
e Mt 8:28
Yoh 5:28
f Mt 27:60
Mk 15:46
g Mk 16:3
Yoh 20:1
h Yoh 9:3
i Mt 14:19
Mk 7:34
j 1Yo 5:14
k Yoh 12:30
l Yoh 6:29
Yoh 17:8
m Lu 7:14
n Mt 27:59
Yoh 20:7

Safu ya 2

a Yoh 2:23
Yoh 10:42
Yoh 12:11
b Lu 16:31
c Zb 2:2
d Hes 14:11
Yoh 7:31
Yoh 12:37
Mdo 4:16
e Yoh 12:19
f Da 9:26
Mdo 28:17
g Mt 24:15
Mdo 6:13
h Mt 26:3
Lu 3:2
Mdo 4:6
i Yoh 18:14
j Lu 2:34
k Isa 49:6
Yak 1:1
1Yo 2:2
l Yoh 17:21
Ga 3:28
Efe 2:14
Efe 3:6
m Mt 26:4
Mt 26:59
Yoh 5:18
n Mt 10:23
Mdo 12:17
o Yoh 7:1
p 2Sa 13:23
2Nya 13:19
q Kut 12:14
Kum 16:1
Yoh 2:13
Yoh 5:1
Yoh 6:4
Yoh 12:1

hiyo mpaka Yerusalemu kabla
ya pasaka kusudi wajitakase
kisherehe.[a] **56** Kwa hiyo wa-
kaenda wakimtafuta Yesu nao
wakawa wakiambiana huku
wakiwa wamesimama kulizu-
nguka hekalu: "Mnaonaje?
Kwamba yeye hatakuja kamwe
kwenye sherehe?" **57** Ilivyo-
kuwa ni kwamba, wakuu wa
makuhani na Mafarisayo wali-
kuwa wametoa maagizo kwa-
mba ikiwa yeyote angepata ku-
jua alikokuwa, anapaswa kufu-
nua hilo, ili wamkamate.

12 Basi, siku sita kabla ya
pasaka, Yesu alifika Be-
thania,[b] alikokuwa Lazaro[c]
ambaye Yesu alikuwa amemfu-
fua kutoka kwa wafu. **2** Kwa
hiyo wakamwandalia mlo wa ji-
oni huko, na Martha[d] aliku-
wa akihudumu,[e] lakini Lazaro
alikuwa mmoja wa wale wali-
okuwa wameketi mezani pa-
moja naye.[f] **3** Kwa hiyo, Ma-
ria akachukua ratili moja ya
mafuta yenye marashi, nardo[g]
halisi, ghali sana, na kuipaka
miguu ya Yesu, naye akaikau-
sha miguu yake kwa kuifuta
kwa nywele zake.[h] Nyumba ika-
jaa harufu ya mafuta yenye ma-
rashi. **4** Lakini Yuda Iskario-
te,[i] mmoja wa wanafunzi wake,
aliyekuwa karibu kumsaliti,
akasema: **5** "Kwa nini mafu-
ta haya yenye marashi[j] hayaku-
uzwa kwa dinari mia tatu na
kupewa maskini?"[k] **6** Inga-
wa hivyo, alisema hilo si kwa
sababu aliwahangaikia maski-
ni, bali kwa sababu yeye alio-
kuwa mwizi[l] na alikuwa na
sanduku la pesa[m] na alikuwa
akichukua pesa zilizowekwa
ndani yake. **7** Kwa hiyo Yesu
akasema: "Mwacheni, ili ashi-
ke mwadhimisho huu kwa ku-
fikiria siku ya maziko yangu.[a]
8 Kwa maana mna maskini[b]
pamoja nanyi sikuzote, lakini
mimi hamtakuwa pamoja nami
sikuzote."

9 Kwa hiyo umati mkubwa
wa Wayahudi wakapata kujua
kwamba alikuwa huko, nao wa-
kaja, si kwa sababu ya Yesu tu,
bali pia wamwone Lazaro, ali-
yemfufua kutoka kwa wafu.[c]
10 Sasa wakuu wa makuhani
wakakata shauri kumuua La-
zaro pia,[d] **11** kwa kuwa we-
ngi kati ya Wayahudi walikuwa
wakienda huko na kumwamini
Yesu[e] kwa sababu yake.

12 Siku iliyofuata umati
mkubwa waliokuwa wameku-
ja kwenye sherehe, waliposi-
kia kwamba Yesu alikuwa aki-
ja Yerusalemu, **13** wakachu-
kua matawi ya mitende[f] na
kutoka nje wakutane naye.
Nao wakaanza kupaaza sau-
ti:[g] "Mwokoe, tunaomba![h]
Aliyebarikiwa ni yule anayeku-
ja katika jina la Yehova,[i] naam,
mfalme[j] wa Israeli!" **14** Laki-
ni Yesu alipompata mwana-pu-
nda,[k] akaketi juu yake, kama
vile ilivyoandikwa: **15** "Usio-
gope, binti Sayuni. Tazama!
Mfalme wako anakuja,[l] akiwa
ameketi juu ya mwana wa pu-
nda."[m] **16** Mambo haya wana-
funzi wake hawakuyajali hapo
kwanza,[n] lakini Yesu alipotu-
kuzwa,[o] ndipo walipokumbuka
kwamba mambo haya yaliku-
wa yameandikwa juu yake na
kwamba walimtendea mambo
hayo.[p]

17 Basi umati uliokuwa pa-
moja naye alipomwita Lazaro[q]

SURA 11

a 2Nya 30:17

SURA 12

b Mk 11:1
c Yoh 11:1
Yoh 11:43
d Lu 10:40
e Mt 27:55
Mk 15:41
f Mt 26:6
Mk 14:3
g Wim 1:12
Mt 26:7
h Lu 7:38
Yoh 11:2
i Mt 26:47
Mk 14:10
Lu 22:48
Yoh 13:29
Mdo 1:16
j Mt 26:8
Mk 14:4
Lu 7:46
k Mt 19:21
Mk 14:5
l Kut 20:15
Met 26:25
m Yoh 13:29

Safu ya 2

a Mt 26:12
Mk 14:8
Yoh 19:40
b Kum 15:11
Mt 26:11
Mk 14:7
c Yoh 11:43
d Met 1:16
Lu 16:31
e Yoh 7:31
Yoh 11:45
f Mt 21:8
Mk 11:8
Ufu 7:9
g Mt 21:9
Mk 11:9
h Zb 118:25
i Zb 118:26
j Yoh 1:49
k 1Fa 1:33
Mt 21:7
Mk 11:7
Lu 19:35
l 1Fa 1:34
m Zek 9:9
n Lu 18:34
o Yoh 7:39
p Lu 24:45
Yoh 14:26
q Yoh 11:1
Yoh 11:43

kutoka kaburini na kumfufua
kutoka kwa wafu ukaendelea
kutoa ushahidi.[a] **18** Kwa aji-
li ya hili umati huo, kwa saba-
bu ulisikia alikuwa amefanya
ishara[b] hiyo, ukakutana naye
pia. **19** Kwa hiyo Mafarisayo[c]
wakasema kati yao wenyewe:
"Ninyi mnaona kwamba ha-
mfanikiwi kamwe. Oneni! Uli-
mwengu umemfuata."[d]

20 Sasa kulikuwa na baadhi
ya Wagiriki[e] kati ya wale wali-
opanda kwenda kuabudu kwe-
nye sherehe. **21** Kwa hiyo,
hao walimkaribia Filipo[f] amba-
ye alikuwa wa kutoka Be-
thsaida ya Galilaya, nao wa-
kaanza kumwomba, wakise-
ma: "Bwana, tunataka kumwo-
na Yesu."[g] **22** Filipo akaja
akamwambia Andrea. Andrea
na Filipo wakaja, wakamwa-
mbia Yesu.

23 Lakini Yesu akawajibu,
akisema: "Saa imekuja Mwa-
na wa binadamu atukuzwe.[h]
24 Kwa kweli kabisa ninawa-
ambia ninyi, Mbegu ya ngano
isipoanguka katika udongo na
kufa, hiyo hubaki ikiwa mbe-
gu moja tu; lakini ikifa,[i] ndi-
po hiyo huzaa matunda mengi.
25 Yule anayeipenda sana
nafsi yake huiangamiza, lakini
yule anayeichukia nafsi[j] yake
katika ulimwengu huu atailin-
da kwa ajili ya uzima wa mi-
lele.[k] **26** Ikiwa yeyote anata-
ka kunihudumia, acha anifua-
te, na mahali nilipo hapo ndipo
mhudumu wangu atakapoku-
wa pia.[l] Ikiwa yeyote anataka
kunihudumia, Baba atamhe-
shimu huyo.[m] **27** Sasa nafsi
yangu inataabika,[n] nami nita-
sema nini? Baba, niokoe kuto-

SURA 12

a Mt 21:15
Lu 19:37
b Yoh 4:54
c Lu 19:39
d Yoh 3:26
Yoh 11:48
Mdo 5:28
e Mdo 17:4
f Yoh 1:44
g Lu 19:3
Lu 23:8
h Yoh 13:32
Yoh 17:1
i Mt 16:21
Ro 14:9
1Ko 15:36
j Mt 10:28
Ufu 12:11
k Mt 16:25
Mk 8:35
Lu 9:24
l Yoh 14:3
Yoh 17:24
1Th 4:17
m 1Sa 2:30
Met 27:18
n Zb 6:3
Mt 26:38
Mk 14:34

Safu ya 2

a Lu 12:50
Lu 22:42
Ebr 5:7
b Mt 3:17
Mt 17:5
Mk 1:11
Mk 9:7
Lu 3:22
Lu 9:35
2Pe 1:17
c Yoh 17:1
d Yoh 11:42
e Yoh 14:30
Yoh 16:11
Mdo 26:18
2Ko 4:4
Efe 2:2
1Yo 5:19
f Lu 10:18
Ufu 12:9
g Yoh 8:28
h Ro 5:18
Ebr 2:9
i Yoh 18:32
Mdo 5:30
j Zb 89:36
Zb 110:4
Isa 9:7
k Yoh 3:14
Yoh 20:9
l Da 7:13
m Yer 13:16
n Yoh 11:10
o Efe 5:8

ka katika saa hii.[a] Hata hivyo,
ndiyo sababu nimekuja kwe-
nye saa hii. **28** Baba, litukuze jina lako." Kwa hiyo sauti[b] ikaja kutoka mbinguni: "Nimelitukuza na pia nitalitukuza tena."[c]

29 Kwa hiyo umati waliosimama huku na huku na kusikia hilo wakaanza kusema kumekuwa na mngurumo. Wengine wakaanza kusema: "Malaika amesema naye." **30** Yesu akajibu, akasema: "Sauti hii imetokea, si kwa ajili yangu, bali kwa ajili yenu.[d] **31** Sasa ulimwengu huu unahukumiwa; sasa mtawala wa ulimwengu[e] huu atatupwa nje.[f] **32** Na bado mimi, nikiinuliwa[g] kutoka duniani, nitavuta watu wa namna zote kwangu."[h] **33** Kwa kweli hili alikuwa akilisema ili kutoa ishara ni kifo cha namna gani alikuwa karibu kufa.[i] **34** Kwa hiyo umati wakamjibu: "Sisi tulisikia kutoka katika Sheria kwamba Kristo hudumu milele;[j] basi kwa nini unasema kwamba lazima Mwana wa binadamu ainuliwe?[k] Huyo Mwana wa binadamu ni nani?"[l] **35** Kwa hiyo Yesu akawaambia: "Nuru itakuwa kati yenu kwa muda kidogo zaidi. Tembeeni wakati mna nuru, ili giza[m] lisiwazidi ngu-
vu; na yule ambaye hutembea katika giza hajui anakoenda.[n] **36** Wakati mna nuru, iweni na imani katika nuru, ili muwe wana wa nuru."[o]

Yesu alisema mambo hayo akaenda zake na kujificha mbali nao. **37** Lakini ijapokuwa alikuwa amefanya ishara nyingi sana mbele yao, hawakuwa

wanamwamini, **38** hata kwa-
mba neno la nabii Isaya likati-
mizwa ambalo alisema: "Yeho-
va, ni nani aliyeliamini jambo
ambalo tumesikia?[a] Na kwa ha-
bari ya mkono wa Yehova, ume-
funuliwa kwa nani?"[b] **39** Wao
hawakuamini kwa sababu tena
Isaya alisema: **40** "Ameyapo-
fusha macho yao naye ameifa-
nya mioyo yao iwe migumu,[c]
ili wasione kwa macho yao
na kulielewa wazo kwa mio-
yo yao na kugeuka nami ni-
waponye."[d] **41** Isaya alisema
mambo haya kwa sababu alio-
na utukufu wake,[e] naye alise-
ma juu yake. **42** Hata hivyo,
wengi hata kati ya watawala
kwa kweli walimwamini,[f] lakini
kwa sababu ya Mafarisayo wa-
kawa hawamkiri, ili wasifuku-
zwe katika sinagogi;[g] **43** kwa
maana waliupenda utukufu wa
wanadamu kuliko hata utukufu
wa Mungu.[h]

44 Hata hivyo, Yesu akapa-
aza sauti na kusema: "Yule
ambaye huniamini huamini, si
mimi tu, bali pia yule aliyeni-
tuma;[i] **45** na yule ambaye hu-
nitazama humtazama pia yule
aliyenituma.[j] **46** Nimekuja
nikiwa nuru ulimwenguni,[k] ili
kila mtu anayeniamini asipate
kukaa katika giza.[l] **47** Lakini
ikiwa yeyote anasikia maneno
yangu na hayashiki, simhuku-
mu; kwa maana nilikuja, si ku-
uhukumu ulimwengu,[m] bali ku-
uokoa ulimwengu.[n] **48** Yule
ambaye hunipuuza wala ha-
pokei maneno yangu ana wa
kumhukumu. Neno[o] ambalo
nimesema ndilo litakalomhu-
kumu katika siku ya mwisho;
49 kwa sababu sijasema ku-

SURA 12

a Ro 10:16
b Isa 53:1
c Kut 4:21
d Isa 6:10
Mt 13:14
Mk 4:12
Mdo 28:27
e Isa 6:1
f Yoh 19:38
g Met 29:25
Yoh 7:13
Yoh 9:22
Yoh 16:2
h Yoh 5:44
Ro 2:29
i Mt 10:40
Mk 9:37
1Pe 1:21
j Yoh 14:9
k Yoh 3:19
Yoh 8:12
Yoh 9:5
l Yoh 12:35
m Yoh 3:17
Yoh 5:45
Yoh 8:15
n Yoh 3:16
o Kum 18:19

Safu ya 2

a Kum 18:18
Yoh 8:38
Yoh 14:10
b Yoh 6:40
Yoh 17:2
c Yoh 3:34

SURA 13

d Mt 26:2
Yoh 12:23
Yoh 16:28
Yoh 17:1
Yoh 17:11
e Yoh 15:9
Yoh 17:9
Ga 2:20
Efe 5:2
1Yo 3:16
f Mt 15:19
Lu 22:3
Yoh 13:27
Mdo 1:25
g Mt 26:16
Mt 26:24
Mk 14:11
h Mt 11:27
Mdo 2:36
1Ko 15:27
Ebr 2:8
i Yoh 16:28
j Flp 2:7
k Mwa 18:4
Lu 7:44
l Lu 9:48
1Pe 5:3
m Yoh 13:12

tokana na msukumo wangu
mwenyewe, bali Baba mwenye-
we aliyenituma amenipa amri
kuhusu jambo la kutangaza na
la kusema.[a] **50** Pia ninajua
kwamba amri yake inamaani-
sha uzima wa milele.[b] Kwa hiyo
mambo ninayosema, kama vile
Baba alivyoniambia, ndivyo ni-
navyoyasema."[c]

13 Sasa, kwa sababu alijua
kabla ya sherehe ya pa-
saka kwamba saa yake ya kuto-
ka katika ulimwengu huu kwe-
nda kwa Baba ilikuwa imefika,[d]
Yesu, akiwa amewapenda wa-
lio wake mwenyewe waliokuwa
ulimwenguni,[e] akawapenda
mpaka mwisho. **2** Kwa
hiyo, mlo wa jioni ulipokuwa
ukiendelea, Ibilisi akiwa ta-
yari ameweka ndani ya moyo
wa Yuda Iskariote,[f] mwana
wa Simoni, amsaliti,[g] **3** yeye,
akijua kwamba Baba aliku-
wa ametia vitu vyote mikono-
ni mwake[h] na kwamba alikuja
kutoka kwa Mungu na alikuwa
akienda kwa Mungu,[i] **4** alisi-
mama kutoka kwenye mlo wa
jioni na kuyaweka kando mava-
zi yake ya nje. Naye akachukua
kitambaa, akajifunga kiuno-
ni.[j] **5** Kisha akatia maji nda-
ni ya beseni akaanza kuiosha
miguu[k] ya wanafunzi na kui-
kausha kwa kitambaa amba-
cho alikuwa amejifunga kiu-
noni. **6** Na kwa hiyo akafika
kwa Simoni Petro. Huyo aka-
mwambia: "Bwana, je, unao-
sha miguu yangu?"[l] **7** Yesu
akajibu, akamwambia: "Ninalo-
fanya huelewi sasa, bali utae-
lewa baada ya mambo haya."[m]
8 Petro akamwambia: "Huta-
osha kamwe miguu yangu."

Yesu akamjibu: "Nisipokuosha,[a] wewe huna sehemu pamoja na mimi." **9** Simoni Petro akamwambia: "Bwana, si
miguu yangu tu, bali pia mikono yangu na kichwa changu."
10 Yesu akamwambia: "Yule
ambaye ameoga[b] hahitaji kuoshwa zaidi ya miguu yake, bali
yuko safi mwili wote. Nanyi
mko safi, lakini si ninyi nyote." **11** Kwa kweli, alimjua
mtu anayemsaliti.[c] Ndiyo sababu alisema: "Si wote kati yenu
walio safi."

12 Basi, alipokuwa ameosha miguu yao na kuvaa mavazi yake ya nje, akaketi mezani tena, akawaambia: "Je,
mnajua jambo ambalo nimewafanyia ninyi? **13** Ninyi hu-
niita, 'Mwalimu,'[d] na, 'Bwana,'[e] nanyi mnasema sawasa-
wa, kwa maana ndivyo nilivyo.[f]
14 Kwa hiyo, ikiwa mimi, ni-
japokuwa Bwana na Mwalimu,
niliiosha miguu yenu,[g] ninyi
pia mnapaswa kuoshana mi-
guu.[h] **15** Kwa maana niliwe-
ka kielelezo kwa ajili yenu, ili,
kama vile nilivyowafanyia ni-
nyi, ninyi pia mfanye hivyo.[i]
16 Kwa kweli kabisa ninawaa-
mbia ninyi, Mtumwa si mkuu
kuliko bwana wake, wala yule
aliyetumwa si mkuu kuliko
yule aliyemtuma.[j] **17** Ikiwa
mnajua mambo haya, wenye fu-
raha ni ninyi ikiwa mnaya-
tenda.[k] **18** Mimi sisemi juu
yenu nyote; ninawajua wale
ambao nimewachagua.[l] Lakini
ni ili Andiko lipate kutimizwa,[m]
'Yule aliyekuwa akila mkate
wangu amekiinua kisigino cha-
ke dhidi yangu.'[n] **19** Kuanzia
dakika hii na kuendelea nina-

SURA 13

a Zb 51:2
1Ko 6:11
Efe 5:26
Tit 3:5
Ebr 10:22
b 2Ko 7:1
Efe 4:22
c Yoh 6:64
d Yoh 1:38
e Lu 2:11
Mdo 10:36
f Mt 23:8
1Ko 8:6
Flp 2:11
g Lu 22:27
h Mt 20:26
Lu 9:48
Lu 22:26
Ro 12:10
Ga 5:13
1Pe 5:5
i Mt 23:3
Flp 2:5
1Pe 2:21
1Yo 2:6
j Mt 10:24
Lu 6:40
Yoh 15:20
k Mt 7:24
Lu 11:28
Yak 1:25
l Yoh 15:16
Efe 1:4
2Th 2:13
2Ti 2:10
m Yoh 17:12
n Zb 41:9
Mt 26:23

Safu ya 2

a Mt 24:25
Yoh 14:29
Yoh 16:4
b Mt 22:3
Ga 4:14
c Mt 10:40
Mt 25:40
d Mt 26:21
Mk 14:18
Lu 22:21
Yoh 6:70
Mdo 1:16
e Mt 26:22
Lu 22:23
f Yoh 19:26
Yoh 20:2
g Yoh 21:20
h Mt 26:23
i Zb 109:6
Lu 22:3
j Yoh 12:6

waambia ninyi kabla ya hilo
kutukia,[a] ili litakapotukia
mwamini kwamba mimi ndiye.
20 Kwa kweli kabisa ninawaa-
mbia, Yule anayempokea ye-
yote ninayemtuma hunipokea
mimi pia.[b] Naye anayenipokea
mimi, humpokea pia yule aliye-
nituma."[c]

21 Baada ya kusema hayo,
Yesu akataabika rohoni, naye
akatoa ushahidi na kusema:
"Kwa kweli kabisa ninawaa-
mbia ninyi, Mmoja wenu ata-
nisaliti."[d] **22** Wanafunzi wa-
kaanza kutazamana, wasijue
kabisa alikuwa akisema hilo
kuhusu nani.[e] **23** Mmoja wa
wanafunzi wake alikuwa amee-
gama kifuani pa Yesu, naye Yesu
alimpenda.[f] **24** Kwa hiyo Si-
moni Petro akamtolea huyo
ishara ya kichwa na kumwa-
mbia: "Muulize anasema hilo
kuhusu nani." **25** Kwa hiyo
huyo wa mwisho akaegemea
nyuma kifuani pa Yesu na ku-
mwambia: "Bwana, ni nani?"[g]
26 Kwa hiyo Yesu akajibu: "Ni
yule ambaye nitampa tonge
ambalo ninachovya."[h] Na kwa
hiyo, akiisha kuchovya tonge,
akalichukua na kumpa Yuda,
mwana wa Simoni Iskariote.
27 Na baada ya hilo tonge ndi-
po Shetani akaingia ndani ya
huyo.[i] Kwa hiyo, Yesu akamwa-
mbia: "Lile unalofanya lifanye
upesi zaidi." **28** Hata hivyo,
hakuna hata mmoja kati ya
wale waliokuwa wameketi me-
zani aliyejua amemwambia hili
kwa nini. **29** Kwa kweli, ba-
adhi yao walikuwa wakifikiri,
kwa kuwa Yuda alikuwa
akilishika sanduku la pesa,[j]
kwamba Yesu alikuwa akimwa-

mbia: "Nunua vitu ambavyo
tunahitaji kwa ajili ya sherehe," au kwamba awape maskini kitu fulani.[a] **30** Kwa hiyo,
baada ya yeye kulipokea tonge,
akatoka nje mara moja, akaenda. Na wakati huo ulikuwa
usiku.[b]

31 Kwa hiyo alipokuwa ameenda, Yesu akasema: "Sasa
Mwana wa binadamu ametukuzwa,[c] na Mungu ametukuzwa
kuhusiana na yeye. **32** Na Mungu mwenyewe atamtukuza,[d]
naye atamtukuza mara moja.
33 Watoto wadogo,[e] nipo pamoja nanyi muda kidogo zaidi. Ninyi mtanitafuta; na kama
vile nilivyowaambia Wayahudi, 'Ninakoenda ninyi hamwezi kuja,'[f] ninawaambia ninyi
pia sasa. **34** Ninawapa ninyi
amri mpya, kwamba mpendane; kama vile ambavyo nimewapenda ninyi,[g] ninyi nanyi mpendane vivyo hivyo.[h] **35** Kwa
jambo hili wote watajua kwamba ninyi ni wanafunzi wangu,
mkiwa na upendo kati yenu wenyewe."[i]

36 Simoni Petro akamwambia: "Bwana, unaenda wapi?"
Yesu akajibu: "Ninakoenda huwezi kunifuata sasa, lakini
utanifuata baadaye."[j] **37** Petro akamwambia: "Bwana, kwa
nini siwezi kukufuata sasa?
Nitatoa nafsi yangu kwa ajili
yako."[k] **38** Yesu akajibu: "Je,
utaitoa nafsi yako kwa ajili yangu? Kwa kweli kabisa ninakuambia, Jogoo hatawika mpaka
uwe umenikana mara tatu."[l]

14 "Mioyo yenu isitaabike.[m]
Iweni na imani katika
Mungu,[n] iweni na imani pia
katika mimi.[o] **2** Katika nyumba ya Baba yangu mna makao
mengi.[a] Kama sivyo, ningaliwaambia ninyi, kwa sababu
ninaenda kuwatayarishia ninyi mahali.[b] **3** Pia, nikienda
na kuwatayarishia ninyi mahali, nitakuja tena[c] nami nitawapokea ninyi nyumbani kwangu
mwenyewe,[d] ili mahali nilipo
mimi, ninyi pia muwe hapo.[e]
4 Na mahali ninakoenda ninyi
mnaijua njia."

5 Tomasi[f] akamwambia:
"Bwana, sisi hatujui unaenda
wapi.[g] Tunaijuaje njia?"

6 Yesu akamwambia: "Mimi
ndiye njia[h] na kweli[i] na uzima.[j]
Hakuna anayekuja kwa Baba
ila kupitia kwangu.[k] **7** Kama
mngekuwa mmenijua, mngekuwa mmemjua Baba yangu
pia; tangu dakika hii na kuendelea ninyi mnamjua na mmemwona."[l]

8 Filipo akamwambia: "Bwana, tuonyeshe Baba, na hilo linatutosha."

9 Yesu akamwambia: "Je, nimekuwa pamoja nanyi kwa
muda mrefu sana hivyo, na
bado, Filipo, hujanijua? Yule
ambaye ameniona mimi amemwona Baba[m] pia. Kwa nini
unasema, 'Tuonyeshe Baba'?[n]
10 Je, wewe huamini kwamba mimi nimo katika muungano pamoja na Baba na
Baba yumo katika muungano
pamoja nami?[o] Mambo ninayowaambia ninyi sisemi kwa kujitungia mwenyewe; bali Baba
ambaye hukaa katika muungano pamoja nami anafanya
kazi zake.[p] **11** Iweni na imani
kwamba nimo katika muungano pamoja na Baba na Baba
yumo katika muungano pamoja

SURA 13
a Mt 19:21
b Mt 26:20
c Yoh 12:23
Yoh 14:13
d Yoh 7:39
Yoh 17:1
e Ebr 2:13
f Yoh 7:34
Yoh 8:21
g Yoh 15:9
Efe 5:2
h Law 19:18
Yoh 15:12
1Th 4:9
Yak 2:8
1Pe 1:22
1Yo 3:14
i Ro 13:8
1Ko 13:8
Ga 6:2
1Yo 4:20
j Yoh 14:3
2Pe 1:14
Ufu 14:4
k Mt 26:33
Mk 14:29
Lu 22:33
l Mt 26:34
Mk 14:30
Lu 22:34
Yoh 18:27

SURA 14
m Yoh 14:27
n Mk 11:22
1Pe 1:21
o Efe 1:13

Safu ya 2
a Lu 16:9
b Lu 12:32
Kol 1:5
1Pe 1:4
c Mdo 1:11
d Yoh 17:24
Ro 8:17
1Ko 15:23
Flp 1:23
1Th 4:16
2Ti 4:8
Ebr 10:19
e 1Th 4:17
f Yoh 11:16
g Yoh 13:36
h Yoh 10:9
Ro 5:2
Efe 2:18
Ebr 10:20
i Yoh 1:17
Ro 15:8
Efe 4:21
Kol 2:17
j Yoh 1:4
Yoh 6:63
Yoh 17:3
Ro 6:23
Ufu 2:10
k Mdo 4:12
l Mt 11:27
Yoh 1:18
Yoh 8:19
1Yo 4:12
m Yoh 5:19
Yoh 8:28
Kol 1:15
Ebr 1:3
n Yoh 12:45
o Yoh 10:38
Yoh 17:21
p Yoh 7:16
Yoh 8:28
Yoh 12:49

nami; kama sivyo, iweni na imani kwa sababu ya zile kazi zenyewe.[a] **12** Kwa kweli kabisa ninawaambia ninyi, Yule anayeniamini, huyo pia atafanya kazi ambazo mimi hufanya; naye atafanya kazi kubwa[b] kuliko hizi, kwa sababu ninaenda kwa Baba.[c] **13** Pia, lolote lile mtakaloomba katika jina langu, nitalifanya, ili Baba apate kutukuzwa kuhusiana na Mwana.[d] **14** Mkiomba jambo lolote katika jina langu, nitalifanya.

15 “Ikiwa mnanipenda, mtazishika amri zangu;[e] **16** nami nitamwomba Baba naye atawapa ninyi msaidizi mwingine awe pamoja nanyi milele,[f] **17** roho ya ile kweli,[g] ambayo ulimwengu hauwezi kuipokea,[h] kwa sababu hauioni wala kuijua. Ninyi mnaijua, kwa sababu hiyo hukaa pamoja nanyi na imo ndani yenu.[i] **18** Sitawaacha ninyi mayatima.[j] Ninakuja kwenu. **19** Bado muda kidogo zaidi na ulimwengu hautaniona tena,[k] lakini ninyi mtaniona,[l] kwa sababu ninaishi, nanyi mtaishi.[m] **20** Siku hiyo mtajua kwamba nimo katika muungano pamoja na Baba yangu nanyi mumo katika muungano pamoja nami, nami nimo katika muungano pamoja nanyi.[n] **21** Yule aliye na amri zangu na kuzishika, huyo ndiye ambaye hunipenda.[o] Naye anayenipenda atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujionyesha wazi kwake.”

22 Yuda,[p] si yule Iskariote, akamwambia: “Bwana, ni nini kimetukia hivi kwamba unakusudia kujionyesha wazi kwetu wala si kwa ulimwengu?”[q]

SURA 14

a Yoh 5:36
b Mt 21:21
Mdo 1:8
Mdo 2:41
Kol 1:23
c Mdo 2:33
d Yoh 15:16
Yoh 16:23
e Yoh 13:34
Yoh 15:10
Yak 1:22
1Yo 5:3
f Lu 24:49
Yoh 15:26
Yoh 16:7
Mdo 1:5
Mdo 2:4
Ro 8:26
g Mt 10:20
Yoh 16:13
1Ko 2:12
1Yo 2:27
h 1Ko 2:14
i Ga 4:6
j Mt 28:20
k Mt 23:39
l Yoh 16:16
Yoh 17:24
m 1Ko 15:22
n Yoh 10:38
Yoh 17:21
o 1Yo 2:5
1Yo 5:1
p Lu 6:16
Mdo 1:13
q Yoh 7:4
Mdo 10:41

Safu ya 2

a Yoh 15:10
b 1Yo 2:24
Ufu 3:20
c Yoh 5:19
Yoh 7:16
Yoh 12:49
d Lu 24:49
Yoh 15:26
Yoh 16:13
1Yo 2:27
e Yoh 16:33
Efe 2:14
Flp 4:7
Kol 3:15
2Th 3:16
f Yoh 20:17
1Ko 11:3
1Ko 15:28
Flp 2:6
g Yoh 13:19
Yoh 16:4
h Yoh 12:31
Yoh 16:11
i Yoh 16:33
j Yoh 10:18
Yoh 12:49
Yoh 15:10
Flp 2:8
1Yo 5:3

SURA 15

k Isa 4:2
l Zb 80:8
Yer 2:21
1Ko 3:9

23 Yesu akajibu, akamwambia: “Ikiwa yeyote ananipenda, atalishika[a] neno langu, na Baba yangu atampenda, nasi hakika tutakuja kwake na kukaa pamoja naye.[b] **24** Yule ambaye hanipendi hayashiki maneno yangu; na neno mnalolisikia si langu, bali ni la Baba aliyenituma.[c]

25 “Nilipokuwa nikikaa pamoja nanyi niliwaambia mambo haya. **26** Lakini msaidizi, roho takatifu, ambayo Baba atatuma katika jina langu, hiyo itawafundisha ninyi mambo yote na kuwakumbusha mambo yote niliyowaambia.[d] **27** Ninawaachia ninyi amani, ninawapa amani[e] yangu. Siwapi ninyi hiyo kwa njia ile ambayo ulimwengu huitoa. Mioyo yenu isitaabike wala kuogopa. **28** Mlisikia kwamba niliwaambia, Ninaenda zangu nami nitakuja tena kwenu. Kama mngenipenda, mngeshangilia kwamba ninaenda kwa Baba, kwa sababu Baba ni mkuu[f] kuliko mimi. **29** Kwa hiyo sasa nimewaambia ninyi kabla ya hilo kutukia,[g] ili, litakapotukia, mpate kuamini. **30** Sitasema mengi tena kamwe pamoja nanyi, kwa maana mtawala[h] wa ulimwengu anakuja. Naye hana uwezo juu yangu,[i] **31** lakini, kusudi ulimwengu ujue kwamba ninampenda Baba, kama vile Baba amenipa amri[j] kufanya, ndivyo ninavyofanya. Simameni, tuondoke hapa.

15 “Mimi ndiye mzabibu wa kweli,[k] na Baba yangu ndiye mkulima.[l] **2** Kila tawi ndani yangu lisilozaa matu-

nda yeye huliondolea mbali,[a]
na kila tawi linalozaa matu-
nda yeye hulisafisha,[b] lipate kuzaa matunda zaidi.[c] **3** Tayari ninyi ni safi kwa sababu ya
neno ambalo nimewaambia.[d]
4 Kaeni katika muungano pa-
moja nami, na mimi katika mu-
ungano pamoja nanyi.[e] Kama
vile tawi lisivyoweza kuzaa
matunda likiwa peke yake li-
sipokaa katika mzabibu, vi-
vyo hivyo ninyi hamwezi, msi-
pokaa katika muungano pamo-
ja nami.[f] **5** Mimi ndiye mza-
bibu, ninyi ndio matawi. Yule
ambaye hukaa katika muunga-
no pamoja nami, na mimi kati-
ka muungano pamoja naye,
huyo huzaa matunda mengi;[g]
kwa sababu bila mimi hamwezi
kufanya lolote kamwe. **6** Iki-
wa yeyote hakai katika muu-
ngano pamoja nami, huyo hu-
tupwa nje kama tawi na hu-
kauka; na watu hukusanya ma-
tawi hayo na kuyatupa ndani
ya moto nayo yanateketezwa.[h]
7 Mkikaa katika muungano
pamoja nami na maneno ya-
ngu yakae ndani yenu, ombeni
lolote mnalotaka nalo litatukia
kwenu.[i] **8** Baba yangu hu-
tukuzwa katika hili, kwamba
mwendelee kuzaa matunda me-
ngi na kujionyesha kuwa wa-
nafunzi wangu.[j] **9** Kama vile
Baba alivyonipenda[k] nami nili-
vyowapenda ninyi, kaeni kati-
ka upendo wangu. **10** Mkishi-
ka amri zangu,[l] mtakaa katika
upendo wangu, kama vile mimi
nilivyoshika amri za Baba[m] na
kukaa katika upendo wake.

11 "Mambo haya nimewaa-
mbia, ili shangwe yangu ipate
kuwa ndani yenu na shangwe

SURA 15

a Mt 15:13
Ebr 6:8
b Efe 5:26
Tit 2:14
1Yo 1:7
1Yo 1:9
c 2Pe 1:8
d Yoh 13:10
Yoh 17:17
Mdo 15:9
1Pe 1:22
e Yoh 6:56
1Ko 12:27
Kol 2:19
f Ga 2:20
Efe 2:21
1Yo 2:6
g Met 11:30
Ho 14:8
Yoh 15:16
Ga 5:22
h Eze 15:4
Mt 3:10
Ro 11:20
Ebr 6:4
Ebr 6:8
1Yo 2:19
i Mt 7:7
Yoh 16:23
j Mt 5:16
Yoh 13:35
Flp 1:11
k Yoh 3:35
l Yoh 13:34
Yoh 14:15
1Yo 2:5
m Yoh 8:29

Safu ya 2

a Yoh 16:24
Yoh 17:13
1Yo 1:4
b Mk 12:31
Yoh 13:34
1Th 4:9
1Pe 4:8
c Yoh 10:11
Ro 5:7
Efe 5:2
1Yo 3:16
d Mt 12:50
Yoh 14:23
e Lu 12:4
f Mdo 20:27
g Mt 28:19
Ro 1:13
Flp 1:22
h Yoh 14:13
i Yoh 13:34
1Yo 3:23
j Mt 10:22
Lu 19:14
Yoh 17:14
1Yo 3:13
k 1Yo 4:5
l Yoh 17:14
Yak 4:4
m Lu 6:22
1Pe 4:4
n Mt 5:11
Mt 10:22
Mt 24:9
2Ti 3:12
1Pe 2:21

yenu ipate kujaa.[a] **12** Hii ndi-
yo amri yangu, kwamba mpe-
ndane kama vile nilivyowape-
nda ninyi.[b] **13** Hakuna aliye
na upendo mkuu kuliko huu,
kwamba mtu aitoe nafsi yake
kwa ajili ya rafiki zake.[c]
14 Ninyi ni rafiki zangu ikiwa
mnafanya ninalowaamuru ni-
nyi.[d] **15** Siwaiti ninyi tena
watumwa, kwa sababu mtu-
mwa hajui yale ambayo bwa-
na wake anafanya. Lakini ni-
mewaita ninyi rafiki,[e] kwa saba-
bu mambo yote ambayo nimeya-
sikia kutoka kwa Baba yangu
nimewajulisha ninyi.[f] **16** Ni-
nyi hamkunichagua mimi, bali
mimi niliwachagua, nami nili-
waweka ninyi msonge mbele
na kuendelea kuzaa matunda[g]
na kwamba matunda yenu ya-
pate kukaa; ili hata mki-
mwomba Baba jambo gani ka-
tika jina langu, apate kuwapa
hilo.[h]

17 "Mambo haya ninawaa-
muru ninyi, kwamba mpendane.[i]
18 Ikiwa ulimwengu unawachu-
kia ninyi, mnajua kwamba ume-
nichukia mimi kabla ya kuwa-
chukia ninyi.[j] **19** Kama mnge-
kuwa sehemu ya ulimwengu,
ulimwengu ungependa kili-
cho chake.[k] Sasa kwa sababu
ninyi si sehemu ya ulimwengu,
bali nimewachagua ninyi ku-
toka ulimwenguni,[l] kwa saba-
bu hiyo ulimwengu unawachu-
kia ninyi.[m] **20** Kumbukeni
neno nililowaambia, Mtumwa
si mkuu kuliko bwana wake.
Ikiwa wamenitesa mimi, wa-
tawatesa ninyi pia;[n] ikiwa wa-
melishika neno langu, watali-
shika lenu pia. **21** Lakini wa-
tawatendea mambo yote haya

kwa ajili ya jina langu, kwa sa-
babu hawamjui aliyenituma.[a]
22 Kama singekuja na kuwa-
ambia, hawangekuwa na dha-
mbi;[b] lakini sasa hawana sababu
ya kujitetea kwa ajili ya dhambi
yao.[c] **23** Anayenichukia ana-
mchukia Baba yangu pia.[d]
24 Kama singefanya kati yao
kazi ambazo hakuna mwingi-
ne aliyezifanya,[e] hawangeku-
wa na dhambi;[f] lakini sasa wa-
meniona na pia wamenichu-
kia mimi na vilevile Baba ya-
ngu.[g] **25** Lakini ni ili neno
lililoandikwa katika Sheria
yao lipate kutimizwa, 'Walini-
chukia bila sababu.'[h] **26** Wa-
kati atakapofika msaidizi amba-
ye nitawapelekea ninyi kuto-
ka kwa Baba,[i] roho ya ile kwe-
li, ambayo inatoka kwa Baba,
huyo atatoa ushahidi juu ya-
ngu;[j] **27** nanyi, mtatoa usha-
hidi,[k] kwa sababu mmekuwa
pamoja nami kutoka wakati ni-
lipoanza.

16 "Nimewaambia ninyi ma-
mbo haya ili msikwazi-
ke.[l] **2** Watu watawafukuza ni-
nyi katika sinagogi.[m] Kwa kwe-
li, saa inakuja wakati ambapo
kila mtu anayewaua ninyi atafi-
kiri amemtolea Mungu utumi-
shi mtakatifu.[n] **3** Lakini wa-
tafanya mambo haya kwa sa-
babu hawamjui Baba wala
hawanijui.[o] **4** Hata hivyo, ni-
mewaambia ninyi mambo haya
ili, saa ya mambo haya itakapo-
fika, mpate kukumbuka niliwa-
ambia mambo haya.[p]

"Hata hivyo, mambo haya si-
kuwaambia hapo kwanza, kwa
sababu nilikuwa pamoja nanyi.
5 Lakini sasa ninaenda kwake
aliyenituma,[q] na bado hakuna
hata mmoja wenu anayeniuli-
za, 'Unaenda wapi?' **6** Lakini
kwa sababu nimewaambia ma-
mbo haya huzuni[a] imejaa mio-
yoni mwenu. **7** Hata hivyo,
ninawaambia ninyi kweli, ni-
naenda zangu kwa faida yenu.
Kwa maana nisipoenda zangu,
msaidizi[b] hatakuja kwenu ka-
mwe; bali nikienda zangu, ni-
tamtuma kwenu. **8** Naye ata-
kapofika ataupa ulimwengu
uthibitisho wenye kusadiki-
sha kuhusu dhambi na kuhusu
uadilifu na kuhusu hukumu:[c]
9 kwanza, kuhusu dhambi,[d]
kwa sababu hawaniamini;[e]
10 kisha kuhusu uadilifu,[f] kwa
sababu ninaenda kwa Baba na-
nyi hamtaniona tena; **11** ki-
sha kuhusu hukumu,[g] kwa sa-
babu mtawala wa ulimwengu
huu amehukumiwa.[h]

12 "Bado nina mambo me-
ngi ya kuwaambia, lakini ha-
mwezi kuyastahimili kwa sasa.[i]
13 Hata hivyo, huyo atakapo-
fika, roho ya ile kweli,[j] ata-
waongoza ninyi ndani ya kweli
yote, kwa maana hatasema
kwa msukumo wake mwe-
nyewe, bali mambo anayoya-
sikia atasema, naye atawa-
tangazia mambo yanayokuja.[k]
14 Huyo atanitukuza,[l] kwa sa-
babu atapokea lililo langu na
kulitangaza kwenu.[m] **15** Yote
aliyo nayo Baba ni yangu.[n] Ndi-
yo sababu nilisema yeye hupo-
kea lililo langu na kulitangaza
kwenu. **16** Baada ya muda ki-
dogo hamtaniona tena,[o] na,
tena, baada ya muda kidogo
mtaniona."

17 Kwa hiyo baadhi ya wa-
nafunzi wake wakaambiana:
"Hili analotuambia linamaani-

SURA 15
a Yoh 16:3
b Yoh 9:41
c Mt 11:21
Ro 1:20
Yak 4:17
d Yoh 5:23
1Yo 2:23
e Mt 11:23
Yoh 7:31
Yoh 11:47
f Yoh 9:41
g Kut 20:5
Yoh 5:42
h Zb 35:19
Zb 69:4
Lu 23:22
i Lu 24:49
Yoh 14:26
j 1Yo 5:6
k Lu 1:2
Lu 24:48
Mdo 1:8
Mdo 2:22
Mdo 5:32
1Pe 5:1

SURA 16
l Mt 11:6
m Yoh 9:22
n Mt 24:9
Mdo 8:1
Mdo 12:2
Mdo 26:11
o Yoh 8:19
Yoh 15:21
Ro 10:2
1Ko 2:8
p Yoh 13:19
Yoh 14:29
q Yoh 7:33
Yoh 13:3

Safu ya 2
a Mt 17:23
Yoh 14:1
Yoh 16:22
b Yoh 14:16
Yoh 14:26
Yoh 15:26
Mdo 2:33
c Yoh 12:48
Mdo 24:25
d Yoh 15:22
Ro 3:20
Ro 7:9
e Yoh 5:38
1Th 2:15
f Isa 42:6
Da 9:24
Ro 4:25
Ro 5:18
g Isa 42:1
Mt 12:18
Yoh 3:18
h Yoh 12:31
Yoh 14:30
i Mk 4:33
1Ko 3:1
j Yoh 16:7
k Mdo 11:28
Mdo 16:6
Mdo 21:11
1Ti 4:1
l 1Yo 4:2
m Yoh 15:26
1Yo 2:27
n Mt 11:27
Yoh 3:35
Yoh 17:10
o Yoh 7:33
Yoh 14:19

sha nini, ‘Baada ya muda kidogo hamtaniona, na, tena, baada ya muda kidogo mtaniona,’ na, ‘kwa sababu ninaenda kwa Baba’?” **18** Kwa hiyo walikuwa wakisema: “Hili analosema linamaanisha nini, ‘muda kidogo’? Sisi hatujui analoongea juu yake.” **19** Yesu alijua[a] walikuwa wanataka kumuuliza, kwa hiyo akawaambia: “Je, mnaulizana kati yenu wenyewe juu ya hili, kwa sababu nilisema, Baada ya muda kidogo hamtaniona, na, tena, baada ya muda kidogo mtaniona? **20** Kwa kweli kabisa ninawaambia, Ninyi mtalia na kuomboleza, bali ulimwengu utashangilia; mtahuzunika,[b] lakini huzuni yenu itageuzwa kuwa shangwe.[c] **21** Mwanamke, anapokuwa akizaa, ana huzuni, kwa sababu saa yake imefika;[d] lakini baada ya kuzaa mtoto mchanga, haikumbuki tena dhiki kwa sababu ya shangwe ya kwamba mtu amezaliwa ulimwenguni. **22** Kwa hiyo, ninyi pia, sasa, kwa kweli, mna huzuni; lakini nitawaona ninyi tena na mioyo yenu itashangilia,[e] na hakuna mtu atakayeichukua shangwe yenu kutoka kwenu. **23** Na siku hiyo[f] hamtaniuliza swali kamwe. Kwa kweli kabisa ninawaambia, Mkimwomba Baba jambo lolote[g] atawapa katika jina langu.[h] **24** Mpaka wakati huu wa sasa ninyi hamjaomba hata jambo moja katika jina langu. Ombeni nanyi mtapokea, ili shangwe yenu ipate kujazwa.[i]

25 “Nimewaambia ninyi mambo haya kwa mifano.[j] Saa inakuja wakati ambapo hakika sitasema nanyi tena kwa mifano, bali nitawaeleza waziwazi kuhusu Baba. **26** Siku hiyo mtaomba katika jina langu, nami siwaambii kwamba nitamwomba Baba kuwahusu ninyi. **27** Kwa maana Baba mwenyewe anawapenda ninyi, kwa sababu mmenipenda[a] na mmeamini kwamba mimi nilitoka nikiwa mwakilishi wa Baba.[b] **28** Mimi nilitoka kwa Baba na nimekuja ulimwenguni. Na zaidi ya hayo, ninauacha ulimwengu nami ninaenda kwa Baba.”[c]

29 Wanafunzi wake wakasema: “Unaona! Sasa unasema waziwazi, nawe husemi kwa mifano. **30** Sasa tunajua kwamba unajua mambo yote[d] na huhitaji kuulizwa swali na yeyote.[e] Kwa hili sisi tunaamini kwamba ulitoka kwa Mungu.”[f] **31** Yesu akawajibu: “Je, mnaamini sasa? **32** Tazameni! Saa inakuja, kwa kweli, imekuja, wakati mtakapotawanyika na kwenda kila mmoja kwenye nyumba[g] yake nanyi mtaniacha peke yangu; na bado siko peke yangu, kwa sababu Baba yuko pamoja nami.[h] **33** Nimewaambia mambo haya ili kupitia kwangu mpate kuwa na amani.[i] Ulimwenguni mna dhiki, lakini jipeni moyo! Mimi nimeushinda ulimwengu.”[j]

17 Yesu alisema mambo haya, akainua macho yake mbinguni,[k] akasema: “Baba, saa imefika; mtukuze mwana wako, ili mwana wako apate kukutukuza wewe,[l] **2** kulingana na vile ambavyo umempa mamlaka juu ya wote wenye mwili,[m] ili, wote ambao

SURA 16
a Yoh 2:25
b Lu 5:35
c Mt 28:8
Lu 24:41
Yoh 20:20
d Mwa 3:16
Isa 26:17
e Lu 24:52
1Pe 1:8
f Yoh 14:20
g Flp 4:6
1Pe 5:7
h Yoh 14:13
Yoh 15:16
1Yo 5:14
i Yoh 15:11
1Yo 1:4
j Mt 13:34
Yoh 10:6

Safu ya 2
a Yoh 14:21
b Yoh 3:13
Yoh 17:8
c 1Fa 8:49
Zb 11:4
Yoh 13:3
Ebr 9:24
d Yoh 21:17
e Yoh 2:25
f Yoh 17:8
g Zek 13:7
Mt 26:31
Mt 26:56
Mk 14:27
h Yoh 8:29
i Yoh 14:27
Efe 2:14
j Mdo 14:22
1Th 3:4
1Yo 4:4
1Yo 5:4
Ufu 3:21

SURA 17
k Mt 14:19
Mk 7:34
Yoh 11:41
l Yoh 12:23
Yoh 13:32
m Da 7:14
Mt 28:18
1Ko 15:25
Flp 2:10
Ebr 2:8

umempa,[a] yeye apate kuwa-
pa uzima wa milele.[b] **3** Uzima
wa milele[c] ndio huu, waendelee
kupata ujuzi[d] juu yako wewe,
Mungu wa pekee wa kweli,[e]
na juu ya yule uliyemtuma,
Yesu Kristo.[f] **4** Nimekutukuza[g]
duniani, nikiwa nimemaliza
kazi ambayo umenipa niifa-
nye.[h] **5** Kwa hiyo sasa wewe,
Baba, nitukuze kando yako
kwa utukufu niliokuwa nao ka-
ndo yako kabla ya ulimwengu
kuwako.[i]

6 "Nimelifunua jina lako
kwa watu ulionipa kutoka uli-
mwenguni.[j] Walikuwa wako,
nawe ukanipa, nao wamelishi-
ka neno lako. **7** Sasa wa-
mejua kwamba yote uliyoni-
pa yametoka kwako; **8** kwa
sababu maneno uliyonipa ni-
mewapa, nao wameyapokea[k]
na wamejua kwamba nilitoka
nikiwa mwakilishi[l] wako, nao
wameamini kwamba uliniti-
uma.[m] **9** Ninaomba juu yao; ni-
nawaombea hao, siuombei uli-
mwengu,[n] bali ninawaombea
wale ambao umenipa; kwa sa-
babu ni wako, **10** na vitu vya-
ngu vyote ni vyako na vyako
ni vyangu,[o] nami nimetukuzwa
kati yao.

11 "Pia, mimi simo tena uli-
mwenguni, bali wao wamo uli-
mwenguni[p] nami ninakuja
kwako. Baba Mtakatifu, walin-
de[q] kwa sababu ya jina lako
ambalo umenipa, ili wawe kitu
kimoja kama vile sisi tulivyo.[r]
12 Nilipokuwa pamoja nao ni-
likuwa nikiwalinda[s] kwa saba-
bu ya jina lako ambalo umeni-
pa; nami nimewatunza, na hata
mmoja wao hakuangamizwa[t]
ila yule mwana wa maanga-

SURA 17

a Yoh 6:37
b Isa 53:11
Yoh 4:14
Yoh 6:27
c Lu 10:25
d Efe 4:13
Flp 1:9
1Ti 6:20
2Pe 3:18
e 1Ko 8:4
1Th 1:9
1Yo 5:20
f Yoh 5:37
g Yoh 13:31
Yoh 14:13
h Yoh 4:34
i Yoh 1:1
Yoh 8:58
Kol 1:15
j Zb 22:22
Yoh 10:29
Mdo 15:14
Ebr 2:12
k Yoh 6:68
Yoh 8:28
Yoh 12:49
Yoh 14:10
l Yoh 16:27
Ebr 3:1
m Yoh 16:30
n 1Yo 5:19
o Yoh 16:15
p Yoh 13:1
q 1Pe 1:5
Yud 24
r Yoh 10:30
Yoh 17:21
s Yoh 6:39
Yoh 10:28
1Yo 5:18
t Yoh 18:9

Safu ya 2

a Mk 14:21
Ebr 10:27
b Zb 41:9
Zb 109:8
Mdo 1:20
c Yoh 15:11
d 1Yo 3:13
e Yoh 8:23
Yoh 15:19
Yak 4:4
f Mt 6:13
2Th 3:3
1Yo 5:18
g Kol 1:13
h Yoh 18:36
i Mdo 15:9
Efe 5:26
1Th 5:23
2Th 2:13
1Pe 1:22
j Flp 2:16
k Zb 12:6
Zb 119:151
Zb 119:160
Yak 1:18
l Yoh 20:21
m 1Th 4:7
Ebr 10:10
n Ro 10:17
1Yo 1:3
o Ro 12:5
1Ko 1:10
Ga 3:28
1Yo 1:7
p Yoh 10:38
Yoh 14:10
q 1Ko 6:17
r Yoh 17:8
s Yoh 14:20
Yoh 17:11
1Yo 1:3
1Yo 3:24
t 1Ko 6:17

mizi,[a] ili andiko lipate kutimi-
zwa.[b] **13** Lakini sasa ninaku-
ja kwako, nami ninasema ma-
mbo haya ulimwenguni ili wao
wapate kuwa na shangwe ya-
ngu ndani yao wenyewe kwa
ukamili.[c] **14** Nimewapa neno
lako, lakini ulimwengu umewa-
chukia,[d] kwa sababu wao si se-
hemu ya ulimwengu, kama vile
ambavyo mimi si sehemu ya uli-
mwengu.[e]

15 "Ninakuomba, si kwamba
uwatoe ulimwenguni, bali uwa-
linde kwa sababu ya yule
mwovu.[f] **16** Wao si sehemu ya
ulimwengu,[g] kama vile amba-
vyo mimi si sehemu ya ulimwe-
ngu.[h] **17** Watakase[i] kwa njia
ya ile kweli; neno[j] lako ni kweli.[k]
18 Kama vile ulivyonituma uli-
mwenguni, vivyo hivyo mimi
pia nimewatuma ulimwenguni.[l]
19 Nami ninajitakasa kwa aji-
li yao, ili wao pia watakaswe[m]
kwa njia ya ile kweli.

20 "Ninawaombea, si hawa
tu, bali pia wale wanaoniami-
ni kupitia neno lao;[n] **21** ili
wote wapate kuwa kitu kimo-
ja,[o] kama vile ambavyo wewe,
Baba, umo katika muunga-
no pamoja na mimi na mimi
nimo katika muungano pamo-
ja na wewe,[p] ili wao pia wapate
kuwa katika muungano pamo-
ja na sisi,[q] ili ulimwengu upa-
te kuamini kwamba uliniti-
uma.[r] **22** Pia, nimewapa utu-
kufu ambao umenipa, ili wa-
pate kuwa kitu kimoja kama
vile sisi tulivyo kitu kimoja.[s]
23 Mimi katika muungano pa-
moja na wao na wewe kati-
ka muungano pamoja na mimi,
ili wapate kukamilishwa kuwa
kitu kimoja,[t] ili ulimwengu upa-

te kujua kwamba wewe ulinituma na kwamba uliwapenda wao kama vile ulivyonipenda mimi. **24** Baba, kwa habari ya kile ambacho umenipa,
ninataka kwamba, mahali nilipo, wao pia wapate kuwa pamoja nami,[a] ili wauone utukufu wangu ambao umenipa, kwa
sababu ulinipenda kabla ya kuwekwa kwa msingi[b] wa ulimwengu.[c] **25** Baba Mwadilifu,[d] kwa kweli, ulimwengu hau-
jakujua wewe;[e] lakini mimi nimekujua, na hawa wamejua kwamba ulinituma.[f] **26** Nami nimewajulisha[g] jina lako nami
nitalijulisha, ili upendo ulionipenda nao upate kuwa ndani yao nami katika muungano pamoja nao."[h]

18 Akiisha kusema mambo hayo, Yesu akaenda pamoja na wanafunzi wake ng'ambo ya mto wa majira ya bari-
di kali wa Kidroni[i] mpaka mahali palipokuwa na bustani, na yeye na wanafunzi wake wakaingia ndani yake.[j] **2** Basi
Yuda pia, msaliti wake, alipajua mahali hapo, kwa sababu nyakati nyingi Yesu alikuwa amekutana hapo pamoja na wa-
nafunzi wake.[k] **3** Kwa hiyo Yuda akachukua kikosi cha askari-jeshi na maofisa wa wakuu wa makuhani na wa Mafa-
risayo nao wakaja hapo wakiwa na mienge na taa na silaha.[l] **4** Kwa hiyo, Yesu akijua mambo yote ambayo yangempa-
ta,[m] akatoka na kuwaambia: "Mnamtafuta nani?" **5** Wakamjibu: "Yesu Mnazareti."[n] Akawaambia: "Mimi ndiye."
Basi Yuda, msaliti[o] wake, alikuwa pia amesimama pamoja nao.

SURA 17
a Lu 22:30
Yoh 12:26
1Th 4:17
b Mwa 4:1
Ebr 4:3
c Yoh 17:5
d Yer 50:7
Ro 3:26
e 1Yo 3:1
f Mt 11:27
Yoh 8:55
Yoh 15:21
g Kum 32:3
Mt 6:9
Yoh 17:6
h Yoh 15:9
Ro 8:39
Efe 3:17

SURA 18
i 2Sa 15:23
j Mt 26:36
Mk 14:32
k Lu 22:39
l Mt 26:47
Mk 14:43
Mdo 1:16
m Yoh 13:3
n Mt 2:23
Mk 1:24
Mk 10:47
Mk 14:67
o Lu 22:47

Safu ya 2
a Yoh 7:46
b Yoh 6:39
Yoh 17:12
c Mt 26:51
Mk 14:47
Lu 22:50
d Mt 26:52
Lu 22:51
Yoh 18:36
e Mt 20:22
Mt 26:42
f Mt 26:57
Lu 3:2
Yoh 18:24
Mdo 4:6
g Yoh 11:50
h Mt 26:58
Mk 14:54
Lu 22:54
i Mt 26:69
Mk 14:66

6 Hata hivyo, alipowaambia: "Mimi ndiye," wakarudi nyuma[a] na kuanguka chini. **7** Kwa
hiyo akawauliza tena: "Mnamtafuta nani?" Wakasema: "Yesu Mnazareti." **8** Yesu akajibu:
"Niliwaambia mimi ndiye. Kwa hiyo, ikiwa ni mimi mnayetafuta, acheni hawa waende"; **9** ili
neno lipate kutimizwa ambalo yeye alisema: "Kati ya wale ambao umenipa sikumpoteza
hata mmoja."[b]

10 Ndipo Simoni Petro, kwa kuwa alikuwa na upanga, akauchomoa na kumpiga mtu-
mwa wa kuhani mkuu, akalikata sikio lake la kuume.[c] Jina la mtumwa huyo lilikuwa Malko.
11 Hata hivyo, Yesu akamwambia Petro: "Tia upanga ndani ya ala yake.[d] Kikombe ambacho
Baba amenipa, je, sipaswi kukinywa?"[e]

12 Basi kikosi cha askari-jeshi na kiongozi wa kijeshi na maofisa wa Wayahudi waka-
mkamata Yesu na kumfunga, **13** nao wakampeleka kwanza kwa Anasi; kwa maana alikuwa
baba-mkwe wa Kayafa, ambaye alikuwa kuhani mkuu mwaka huo.[f] **14** Kwa kweli, Kayafa
ndiye aliyewashauri Wayahudi kwamba ilikuwa kwa faida yao mtu mmoja afe kwa ajili ya
watu.[g]

15 Sasa Simoni Petro na vilevile mwanafunzi mwingine alikuwa akimfuata Yesu.[h] Mwa-
nafunzi huyo alijulikana na kuhani mkuu, naye akaingia pamoja na Yesu ndani ya ua wa
kuhani mkuu, **16** lakini Petro alikuwa amesimama nje kwenye mlango.[i] Kwa hiyo yule mwanafunzi mwingine,

ambaye alijulikana na kuhani
mkuu, akatoka nje na kusema
na mtunza-mlango, akamwingiza Petro ndani. **17** Basi kija-
kazi, aliye mtunza-mlango, aka-
mwambia Petro: "Wewe pia ni
mmoja wa wanafunzi wa mtu
huyu, sivyo?" Akasema: "Ha-
pana."[a] **18** Sasa wale watu-
mwa na maofisa walikuwa wa-
mesimama huku na huku, kwa
kuwa walikuwa wamewasha
moto wa makaa,[b] kwa sababu
kulikuwa na baridi, nao walikuwa wakiota moto. Petro pia alikuwa amesimama pamoja nao akiota moto.

19 Na kwa hiyo mkuu wa
makuhani akamuuliza Yesu juu
ya wanafunzi wake na juu ya fundisho lake. **20** Yesu akamjibu: "Nimesema na ulimwengu
hadharani. Sikuzote nilifundi-
sha katika sinagogi na katika hekalu,[c] ambapo Wayahudi
wote hukusanyika; nami siku-
sema jambo lolote katika
siri. **21** Kwa nini unaniuliza?
Waulize wale ambao wamesi-
kia lile nililowaambia. Ona!
Hawa wanajua lile nililosema."
22 Baada ya kusema mambo
hayo, mmoja wa maofisa ali-
yekuwa amesimama kando
akampiga Yesu kofi[d] usoni na
kusema: "Je, hivyo ndivyo una-
vyomjibu mkuu wa makuha-
ni?" **23** Yesu akamjibu: "Iki-
wa nimesema vibaya, toa usha-
hidi kuhusu ubaya wenyewe;
lakini ikiwa nimesema sawa-
sawa, kwa nini unanipiga?"
24 Basi Anasi akaagiza apele-
kwe kwa Kayafa kuhani mkuu[e]
akiwa amefungwa.

25 Sasa Simoni Petro aliku-
wa amesimama akiota moto.

SURA 18

a Mk 14:68
Yoh 18:25

b Yer 36:22

c Mt 26:55
Lu 4:15
Lu 19:47
Yoh 7:14

d Isa 50:6
Mt 5:39
Yoh 19:3
Mdo 23:2

e Mt 26:57

Safu ya 2

a Mt 26:69
Mk 14:69
Lu 22:58

b Yoh 18:10

c Mt 26:74
Mk 14:72
Lu 22:60
Yoh 13:38

d Mt 27:2
Mk 15:1
Lu 23:1
Mdo 3:13

e Mdo 10:28

f Lu 23:2

g Yoh 19:6
Mdo 18:15

h Yoh 19:10

i Mt 20:19
Yoh 3:14
Yoh 12:32

j Mt 27:11
Yoh 12:13

k Yoh 18:29

Ndipo wakamwambia: "Wewe
pia ni mmoja wa wanafunzi
wake, sivyo?" Akakana na
kusema: "Hapana."[a] **26** Mmo-
ja wa watumwa wa kuhani
mkuu, akiwa ni jamaa ya mtu
ambaye Petro alikata sikio
lake,[b] akasema: "Mimi nilikuo-
na katika bustani pamoja naye,
sivyo?" **27** Hata hivyo, Petro
akakana tena; na mara jogoo
akawika.[c]

28 Basi wakampeleka Yesu
kutoka kwa Kayafa mpaka
kwenye jumba la gavana.[d] Sasa
ilikuwa asubuhi. Lakini wao
wenyewe hawakuingia ndani
ya jumba la gavana, ili wasi-
pate kutiwa unajisi[e] bali wapa-
te kula pasaka. **29** Kwa hiyo
Pilato akawajia nje na kusema:
"Ni shtaka gani ambalo mnale-
ta juu ya mtu huyu?"[f] **30** Wa-
kamwambia: "Kama mtu huyu
hangekuwa mkosaji, hatu-
ngemtia mkononi mwako."
31 Kwa sababu hiyo Pilato aka-
waambia: "Mchukueni ninyi
wenyewe na kumhukumu kuli-
ngana na sheria yenu."[g] Waya-
hudi wakamwambia: "Si hala-
li kwetu kumuua mtu yeyote."[h]
32 Kusudi neno la Yesu litimi-
zwe alilosema ili kutoa ishara
ni kifo cha namna gani amba-
cho angekufa.[i]

33 Kwa hiyo Pilato akaingia
tena ndani ya jumba la gavana
naye akamwita Yesu na kumwa-
mbia: "Je, wewe ndiye mfalme
wa Wayahudi?"[j] **34** Yesu aka-
jibu: "Je, jambo unalosema ume-
jitungia mwenyewe, au wengi-
ne walikuambia juu yangu?"[k]
35 Pilato akajibu: "Je, mimi ni
Myahudi? Taifa lako mwenye-
we na wakuu wa makuhani wa-

likutia mikononi mwangu.[a] Ulifanya nini?" **36** Yesu akajibu:[b] "Ufalme wangu si sehemu ya ulimwengu huu.[c] Kama ufalme wangu ungekuwa sehemu ya ulimwengu huu, watumishi wangu wangepigana[d] ili nisitiwe mikononi mwa Wayahudi. Lakini, kama ilivyo, ufalme wangu hautoki katika chanzo hiki." **37** Kwa hiyo Pilato akamwambia: "Kwa hiyo, basi, je, wewe ni mfalme?" Yesu akajibu: "Wewe mwenyewe unasema kwamba mimi ni mfalme.[e] Kwa ajili ya hili mimi nimezaliwa, na kwa ajili ya hili nimekuja ulimwenguni, ili nitoe ushahidi juu ya ile kweli.[f] Kila mtu aliye upande wa ile kweli[g] huisikiliza sauti yangu."[h] **38** Pilato akamwambia: "Kweli ni nini?"

Na baada ya kusema hili, akatoka tena kwenda kwa Wayahudi na kuwaambia: "Mimi sioni kosa lolote ndani yake.[i] **39** Zaidi ya hayo, ninyi mna desturi kwamba niwafungulie mtu kwenye pasaka.[j] Kwa hiyo, je, mnataka niwafungulie mfalme wa Wayahudi?" **40** Basi wakapaaza sauti tena, wakisema: "Si mtu huyu, bali Baraba!" Basi Baraba alikuwa mnyang'anyi.[k]

19 Kwa hiyo, wakati huo Pilato akamchukua Yesu na kumpiga mijeledi.[l] **2** Nao askari-jeshi wakasokota taji la miiba na kuliweka juu ya kichwa chake nao wakampamba kwa vazi la nje la zambarau;[m] **3** nao wakaanza kumjia na kusema: "Siku njema, ewe Mfalme wa Wayahudi!" Pia wakawa wakimpiga makofi usoni.[n]

SURA 18
a Yoh 1:11
b 1Ti 6:13
c Isa 9:6
Da 2:44
Da 7:14
d Mt 26:53
Yoh 18:11
e Mt 26:64
Mt 27:11
f Yoh 1:14
Yoh 1:17
Yoh 14:6
g Yoh 8:32
1Yo 3:19
1Yo 4:6
h Yoh 8:46
i Mt 27:24
Lu 23:4
Yoh 15:25
j Mt 27:15
Mk 15:6
k Hes 35:31
Lu 23:19
Mdo 3:14

SURA 19
l Isa 50:6
Mt 20:19
Mt 27:26
Mk 15:15
Lu 18:33
m Mt 27:29
Mk 15:17
Lu 23:11
n Isa 53:3

Safu ya 2
a Lu 23:4
Yoh 18:38
2Ko 5:21
b Kut 23:7
Mt 27:22
Mk 15:13
Lu 23:21
c Yoh 18:31
Mdo 3:13
d Law 24:16
e Mt 26:63
Yoh 5:18
f Isa 53:7
Mt 27:12
Mt 27:14
Mdo 8:32
g Lu 23:9
h Mwa 45:8
Da 4:17
Lu 22:53
Yoh 7:30
Yoh 10:18
Ro 13:2
Ufu 13:7
i Lu 23:2
Mdo 17:7

4 Naye Pilato akaenda nje tena na kuwaambia: "Oneni! Namleta nje kwenu kusudi mjue kwamba sioni kosa lolote ndani yake."[a] **5** Basi Yesu akaja nje, akiwa amevaa taji lenye miiba na vazi la nje la zambarau. Naye akawaambia: "Tazameni! Mwanamume!" **6** Hata hivyo, wakuu wa makuhani na maofisa walipomwona, wakapaaza sauti, wakisema: "Mtundike mtini! Mtundike mtini!"[b] Pilato akawaambia: "Mchukueni ninyi wenyewe mkamtundike mtini, kwa maana mimi sioni kosa lolote ndani yake."[c] **7** Wayahudi wakamjibu: "Sisi tuna sheria,[d] na kulingana na sheria anapaswa kufa, kwa sababu alijifanya mwenyewe kuwa mwana wa Mungu."[e]

8 Kwa hiyo, Pilato aliposikia maneno hayo, akaogopa zaidi; **9** naye akaingia ndani ya jumba la gavana tena na kumwambia Yesu: "Wewe ni mtu wa kutoka wapi?" Lakini Yesu hakumjibu.[f] **10** Kwa sababu hiyo Pilato akamwambia: "Je, husemi nami?[g] Je, hujui nina mamlaka ya kukufungua na nina mamlaka ya kukutundika mtini?" **11** Yesu akamjibu: "Wewe hungekuwa na mamlaka hata kidogo juu yangu kama usingepewa kutoka juu.[h] Ndiyo sababu mtu aliyenitia mikononi mwako ana dhambi kubwa zaidi."

12 Kwa sababu hii Pilato akazidi kutafuta jinsi ya kumfungua. Lakini Wayahudi wakapaaza sauti, wakisema: "Ukimfungua mtu huyu, wewe si rafiki ya Kaisari. Kila mtu anayejifanya mfalme anasema vibaya juu ya Kaisari."[i]

13 Kwa hiyo Pilato, baada ya
kusikia maneno hayo, akamle-
ta Yesu nje, naye akaketi juu
ya kiti cha hukumu mahali pa-
napoitwa Sakafu ya Jiwe, laki-
ni, katika Kiebrania, *Gabatha.*
14 Sasa kulikuwa na mataya-
risho[a] ya pasaka; karibu saa
sita. Naye akawaambia Waya-
hudi: "Oneni! Mfalme wenu!"
15 Hata hivyo, wakapaaza sau-
ti: "Mwondolee mbali! Mwondo-
lee mbali! Mtundike mtini!" Pi-
lato akawaambia: "Je, nimtu-
ndike mtini mfalme wenu?"
Wakuu wa makuhani wakajibu:
"Sisi hatuna mfalme ila Kaisa-
ri."[b] **16** Kwa hiyo, wakati huo
akamtia mikononi mwao, wa-
kamtundike mtini.[c]

Basi wakamchukua Yesu.
17 Naye, akajibebea mti wa ma-
teso,[d] akaenda[e] pale panapoi-
twa Mahali pa Fuvu la Kichwa,
panapoitwa *Golgotha* katika
Kiebrania;[f] **18** na huko waka-
mtundika mtini,[g] na watu we-
ngine wawili pamoja naye,
mmoja upande huu na mmoja
upande huu, lakini Yesu katika-
ti.[h] **19** Pilato akaandika pia
tangazo na kuliweka juu ya huo
mti wa mateso. Liliandikwa:
"Yesu Mnazareti Mfalme wa
Wayahudi."[i] **20** Kwa hiyo we-
ngi wa Wayahudi walilisoma ta-
ngazo hilo, kwa sababu mahali
ambapo Yesu alitundikwa pali-
kuwa karibu na jiji;[j] nalo lilia-
ndikwa kwa Kiebrania, kwa Ki-
latini, kwa Kigiriki. **21** Hata
hivyo, wakuu wa makuhani
wa Wayahudi wakaanza ku-
mwambia Pilato: "Usiandike
'Mfalme wa Wayahudi,' bali
kwamba alisema, 'Mimi ni Mfa-
lme wa Wayahudi.'" **22** Pila-
to akajibu: "Yale ambayo nime-
andika, nimeandika."

23 Sasa wakati askari-jeshi
walipokuwa wamemtundika
Yesu mtini, wakachukua ma-
vazi yake ya nje na kufanya
sehemu nne, kwa kila askari-je-
shi sehemu moja, na vazi la nda-
ni. Lakini lile vazi la ndani lili-
kuwa halina mshono, likiwa li-
mefumwa kutoka juu mpaka
urefu wake wote.[a] **24** Kwa
hiyo wakaambiana: "Tusilira-
rue, bali na tuamue kwa kura
juu yake litakuwa la nani." Hii
ilikuwa ili andiko lipate kutimi-
zwa: "Waligawana mavazi ya-
ngu ya nje, nalo vazi langu wali-
lipigia kura."[b] Ndivyo hasa hao
askari-jeshi walivyofanya ma-
mbo hayo.

25 Hata hivyo, kando ya mti
wa mateso wa Yesu, walikuwa
wamesimama mama[c] yake na
dada ya mama yake; Maria[d] mke
wa Klopa, na Maria Magdale-
ne.[e] **26** Kwa hiyo Yesu, alipo-
mwona mama yake na mwana-
funzi ambaye alimpenda[f] wa-
mesimama kando, akamwambia
mama yake: "Mwanamke, ona!
Mwana wako!" **27** Halafu aka-
mwambia mwanafunzi huyo:
"Ona! Mama yako!" Na tangu
saa hiyo na kuendelea mwa-
nafunzi huyo akampeleka nyu-
mbani kwake.

28 Baada ya hayo, Yesu ali-
pojua kwamba kufikia sasa ma-
mbo yote yalikuwa yametimi-
zwa, ili andiko lipate kutimi-
zwa, akasema: "Nina kiu."[g]
29 Chombo kimoja kilichojaa
divai kali kilikuwa hapo. Kwa
hiyo wakaweka sifongo iliyo-
jaa divai kali juu ya kijiti cha
hisopo na kukileta kwenye ki-

SURA 19
a Mt 27:62
Yoh 19:31
b Mwa 49:10
Kum 17:15
c Kut 23:2
Da 9:27
Mt 27:26
Mt 27:31
Mk 15:15
Lu 23:24
d Mwa 22:6
Mt 27:32
e Law 16:27
Ebr 13:12
f Mt 27:33
Mk 15:22
g Yoh 3:14
Mdo 5:30
2Ko 5:21
Ga 3:13
h Isa 53:9
Lu 23:33
i Mt 27:37
Mk 15:26
Lu 23:38
j Ebr 13:12

Safu ya 2
a Mt 27:35
Mk 15:24
Lu 23:34
b Zb 22:18
c Lu 2:34
d Mt 27:61
e Mt 27:56
Mk 15:40
Lu 23:49
f Yoh 13:23
Yoh 21:7
Yoh 21:20
g Zb 22:15

nywa chake.[a] **30** Sasa, alipo-
kuwa amepokea ile divai kali,
Yesu akasema: "Imetimizwa!"[b]
na, akiinamisha kichwa chake,
akaitoa roho yake.[c]

31 Basi Wayahudi, kwa
kuwa yalikuwa ni Matayari-
sho,[d] ili miili hiyo isipate ku-
kaa[e] juu ya miti ya mateso siku
ya Sabato, (kwa maana siku ya
Sabato hiyo ilikuwa kuu,)[f] wa-
kamwomba Pilato aagize mi-
guu yao ivunjwe na miili io-
ndolewe. **32** Kwa hiyo, askari-
jeshi wakaja na kuvunja mi-
guu ya mtu wa kwanza na ile
ya yule mtu mwingine aliyeku-
wa ametundikwa mtini pamo-
ja naye. **33** Lakini walipoku-
ja kwa Yesu, kwa kuwa wali-
ona kwamba tayari alikuwa
amekufa, hawakuivunja mi-
guu yake. **34** Lakini mmoja
wa hao askari-jeshi akaucho-
ma ubavu wake kwa mkuki,[g]
na mara moja damu na maji vi-
katoka. **35** Na yeye ambaye
ameona hilo ametoa ushahidi,
nao ushahidi wake ni wa kwe-
li, na mtu huyo anajua kwamba
yeye husema mambo ya kwe-
li, ili ninyi pia mweze kuamini.[h]
36 Kwa kweli, mambo haya ya-
litendeka kusudi andiko liti-
mizwe: "Hakuna mfupa wake
hata mmoja utakaovunjwa."[i]
37 Na, tena, andiko tofauti li-
nasema: "Watamtazama Yule
waliyemchoma."[j]

38 Basi baada ya mambo
haya Yosefu kutoka Arima-
thea, aliyekuwa mwanafunzi
wa Yesu lakini kwa siri kwa
sababu alikuwa akiwaogopa
Wayahudi,[k] alimwomba Pilato
apate kuondoa mwili wa Yesu;
naye Pilato akampa ruhusa.[l]

SURA 19
a Zb 69:21
Mt 27:48
Mk 15:36
Lu 23:36
b Yoh 17:4
c Zb 104:29
Isa 53:12
Mt 27:50
Mk 15:37
Lu 23:46
d Mt 27:62
Yoh 19:14
e Kum 21:23
f Law 23:7
g Isa 53:5
Zek 12:10
Mt 27:49
Yoh 20:25
Ufu 1:7
h Yoh 20:31
Yoh 21:24
1Yo 1:1
i Kut 12:46
Hes 9:12
Zb 34:20
j Zek 12:10
Ufu 1:7
k Met 29:25
Yoh 7:13
Yoh 9:22
l Mt 27:58
Mk 15:43
Lu 23:50

Safu ya 2
a Kum 21:23
b 2Nya 16:14
Lu 23:56
Yoh 7:50
c Yoh 20:7
d Isa 53:9
Mdo 13:29
e Mt 27:62
Yoh 19:14

SURA 20
f Law 23:11
1Ko 15:20
g Mt 28:1
Mk 16:1
Lu 24:1
h Yoh 13:23
Yoh 19:26
Yoh 21:24
i Yoh 19:41
j Lu 24:12
k Yoh 19:40

Kwa hiyo akaja na kuuondoa
mwili wake.[a] **39** Nikodemo
pia, yule mtu aliyemjia usiku
mara ya kwanza, akaja akile-
ta msokoto wa manemane na
udi, karibu ratili mia moja.[b]
40 Basi wakauchukua mwili
wa Yesu na kuufunga kwa vi-
tambaa pamoja na manukato,[c]
sawa na jinsi Wayahudi walivyo
na desturi ya kutayarisha kwa
ajili ya maziko. **41** Ilitukia
kwamba, mahali alipotundi-
kwa mtini palikuwa na bustani,
na katika bustani hiyo kaburi ji-
pya,[d] ambalo bado hakuna ye-
yote aliyekuwa amelazwa nda-
ni yake. **42** Basi, kwa saba-
bu ya matayarisho[e] ya Wayahu-
di, wakamlaza Yesu humo, kwa
kuwa kaburi hilo lilikuwa hapo
karibu.

20 Siku ya kwanza[f] ya juma
Maria Magdalene akaja
mapema kwenye kaburi, kuli-
pokuwa na giza bado, naye aka-
ona jiwe likiwa tayari limeo-
ndolewa kutoka kwenye kabu-
ri.[g] **2** Kwa hiyo akakimbia na
kuja kwa Simoni Petro na kwa
yule mwanafunzi[h] mwingine,
ambaye Yesu alikuwa anampe-
nda, naye akawaambia: "Wame-
mwondoa Bwana kutoka kati-
ka kaburi,[i] nasi hatujui wame-
mlaza wapi."

3 Ndipo Petro[j] na yule mwa-
nafunzi mwingine wakato-
ka kwenda kaburini. **4** Ndi-
yo, hao wawili pamoja wa-
kaanza kukimbia; lakini yule
mwanafunzi mwingine aka-
kimbia mbele ya Petro mbio
zaidi naye akafika kaburini
kwanza. **5** Naye akainama,
akaona vitambaa vikiwa chi-
ni humo,[k] lakini hakuingia.

6 Ndipo Simoni Petro pia akaja akimfuata, naye akaingia
ndani ya kaburi. Naye akaona
vitambaa vikiwa chini humo,[a]
7 pia nguo iliyokuwa juu ya
kichwa chake haikuwapo pa-
moja na vitambaa bali ilikuwa
imekunjwa ikiwa peke yake.
8 Kwa hiyo, wakati huo mwa-
nafunzi yule mwingine aliye-
kuwa amefika kwanza kwenye
kaburi akaingia pia, naye aka-
ona na kuamini. **9** Kwa maa-
na bado hawakufahamu andiko
kwamba lazima afufuliwe ku-
toka kwa wafu.[b] **10** Na kwa
hiyo wanafunzi wakarudi nyu-
mbani kwao.

11 Hata hivyo, Maria akaen-
delea kusimama nje karibu
na kaburi, akilia. Ndipo, alipo-
kuwa akilia, akainama kutaza-
ma ndani ya kaburi **12** naye
akaona malaika[c] wawili wali-
okuwa wamevaa mavazi me-
upe wakiwa wameketi mmoja
kichwani na mwingine mi-
guuni ambapo mwili wa Yesu
ulikuwa umelazwa. **13** Nao
wakamwambia: "Mwanamke,
kwa nini unalia?" Akawaa-
mbia: "Wamemwondoa Bwa-
na wangu, nami sijui wame-
mlaza wapi." **14** Baada ya ku-
sema hayo, akageuka na
kumwona Yesu akiwa amesi-
mama, lakini hakufahamu ni
Yesu.[d] **15** Yesu akamwambia:
"Mwanamke, kwa nini unalia?
Unamtafuta nani?"[e] Yeye, aki-
waza ni mtunza-bustani, aka-
mwambia: "Bwana, ikiwa ume-
mchukua, niambie umemla-
za wapi, nami nitamwondoa."
16 Yesu akamwambia: "Ma-
ria!"[f] Alipogeuka, Maria aka-
mwambia, katika Kiebrania:
"Raboni!"[a] (ambalo linama-
anisha "Mwalimu!") **17** Yesu
akamwambia: "Acha kuning'a-
ng'ania. Kwa maana bado sija-
panda kwenda kwa Baba. La-
kini nenda kwa ndugu[b] zangu,
nawe uwaambie, 'Mimi nina-
panda kwenda kwa Baba[c] ya-
ngu na Baba yenu na kwa Mu-
ngu wangu[d] na Mungu wenu.'"[e]
18 Maria Magdalene akaja na
kuleta habari hizo kwa wanafu-
nzi: "Nimemwona Bwana!" na
kwamba alimwambia mambo
hayo.[f]

19 Kwa hiyo, ilipokuwa jio-
ni-jioni siku hiyo, siku ya
kwanza ya juma,[g] na, ijapoku-
wa milango ilikuwa imefungwa
mahali ambamo wanafunzi wa-
likuwa kwa sababu ya kuwao-
gopa[h] Wayahudi, Yesu alikuja[i]
na kusimama katikati yao na
kuwaambia: "Na muwe na amani."[j]
20 Na baada ya kusema
hayo, akawaonyesha miko-
no yake miwili na ubavu wake.[k]
Basi wanafunzi hao wakasha-
ngilia[l] kwa kumwona Bwana.
21 Kwa hiyo, Yesu akawaa-
mbia tena: "Na muwe na amani.
Kama vile ambavyo Baba ame-
nituma,[m] mimi pia ninawatu-
ma ninyi."[n] **22** Na baada ya
kusema jambo hilo akapuliza
juu yao na kuwaambia: "Poke-
eni roho takatifu.[o] **23** Mkisa-
mehe dhambi za watu wowo-
te,[p] watakuwa wamesamehe-
wa; msiposamehe zile za watu
wowote, watakuwa hawajasa-
mehewa."[q]

24 Lakini Tomasi,[r] mmoja
wa wale kumi na wawili, ali-
yeitwa Pacha, hakuwa pamoja
nao Yesu alipokuja. **25** Kwa
hiyo wanafunzi wengine wa-

SURA 20
a Yoh 11:44
b Zb 16:10
Isa 53:10
Mt 16:21
Yoh 2:22
Mdo 2:27
1Ko 15:4
c Mk 16:5
Ebr 1:14
Ufu 19:14
d Lu 24:16
Lu 24:31
Yoh 21:4
e Yoh 1:38
f Yoh 10:3

Safu ya 2
a Mk 10:51
Yoh 1:38
b Zb 22:22
Mt 12:50
Mt 25:40
Mt 28:10
Ro 8:29
Ebr 2:11
c Yoh 14:28
Yoh 16:28
d 1Ko 11:3
Efe 1:17
Kol 1:3
e Mwa 17:7
Ebr 11:16
f Mt 28:10
Lu 24:10
g Lu 24:1
h Yoh 9:22
i 1Ko 15:5
j Mt 10:12
Lu 10:5
Lu 24:36
k Yoh 19:34
1Yo 1:1
l Yoh 16:22
m Isa 61:1
Yoh 5:36
n Mt 28:19
Yoh 17:18
2Ti 2:2
o Lu 1:67
Lu 2:25
Mdo 2:2
Mdo 2:4
p Mt 16:19
q Mdo 13:11
r Yoh 11:16

kawa wanamwambia: "Tume-
mwona Bwana!" Lakini yeye
akawaambia: "Nisipoona kati-
ka mikono yake alama ya mi-
sumari na nitie kidole changu
katika alama ya misumari na
kuutia mkono wangu ndani ya
ubavu wake,[a] hakika mimi sita-
amini."[b]
26 Basi, siku nane baadaye
wanafunzi wake walikuwa
tena ndani ya nyumba, naye
Tomasi alikuwa pamoja nao.
Yesu akaja, ijapokuwa mila-
ngo ilikuwa imefungwa, naye
akasimama katikati yao, aka-
sema: "Na muwe na amani."[c]
27 Halafu akamwambia Toma-
si: "Weka kidole chako hapa,
uone mikono yangu, na chu-
kua mkono[d] wako utie nda-
ni ya ubavu wangu, na ua-
che kuwa asiyeamini bali uwe
mwenye kuamini." **28** Toma-
si akajibu akamwambia: "Bwa-
na wangu na Mungu wangu!"[e]
29 Yesu akamwambia: "Kwa
sababu umeniona je, umeamini?
Wenye furaha ni wale ambao
hawaoni na bado wanaamini."[f]
30 Kwa hakika, Yesu alifa-
nya pia ishara nyingine nyi-
ngi mbele ya wanafunzi hao,
ambazo hazikuandikwa ka-
tika kitabu hiki cha kuku-
njwa.[g] **31** Lakini haya yame-
andikwa[h] ili mpate kuami-
ni kwamba Yesu ndiye Kristo
Mwana wa Mungu, na kwamba,
kwa sababu ya kuamini,[i] mpa-
te kuwa na uzima kupitia jina
lake.

21 Baada ya mambo haya
Yesu alijifunua tena kwa
wanafunzi kwenye bahari ya
Tiberia; lakini alijifunua hivi.
2 Waliokuwa pamoja ni Simo-
ni Petro na Tomasi, aliyeitwa
Pacha,[a] na Nathanaeli[b] kutoka
Kana ya Galilaya na wana wa
Zebedayo[c] na wengine wawili
kati ya wanafunzi wake. **3** Si-
moni Petro akawaambia: "Ni-
naenda kuvua samaki." Waka-
mwambia: "Sisi pia tutakwenda
pamoja nawe." Wakatoka kwe-
nda, wakapanda ndani ya ma-
shua, lakini usiku huo hawaku-
vua kitu.[d]
4 Hata hivyo, ilipokuwa tu
inakaribia kuwa asubuhi, Yesu
akasimama pwani, lakini wana-
funzi, bila shaka, hawakufaha-
mu kwamba ni Yesu.[e] **5** Basi
Yesu akawaambia: "Watoto, je,
mna chakula chochote?" Waka-
mjibu: "Hapana!" **6** Akawaa-
mbia: "Utupeni wavu upande
wa kuume wa mashua, nanyi
mtapata."[f] Basi wakautupa,
lakini hawakuweza tena ku-
uvuta ndani kwa sababu sa-
maki walikuwa wengi sana.[g]
7 Kwa hiyo mwanafunzi amba-
ye Yesu alikuwa akimpenda,[h]
akamwambia Petro:[i] "Ni Bwa-
na!" Kwa hiyo Simoni Petro, ali-
posikia kwamba ni Bwana, aka-
jifunga mwenyewe kwa kuji-
zungushia kiunoni vazi lake la
juu, kwa maana alikuwa uchi,
akajitumbukiza ndani ya baha-
ri. **8** Lakini wale wanafunzi
wengine wakaja katika ile ma-
shua ndogo, kwa maana hawa-
kuwa mbali na nchi kavu, kari-
bu umbali wa meta 90 tu, wa-
kiukokota wavu wenye samaki
wengi.
9 Hata hivyo, waliposhuka
kwenye nchi kavu wakaona
moto wa makaa[j] na samaki juu
yake na mkate. **10** Yesu aka-
waambia: "Leteni baadhi ya

SURA 20
a Yoh 19:34
b 2Ko 5:7
c Yoh 20:19
d 1Yo 1:1
e Isa 9:6
Yoh 1:1
Yoh 1:18
Yoh 14:28
Yoh 20:17
Yoh 20:31
f 2Ko 5:7
1Pe 1:8
g Yoh 21:25
h Lu 1:4
i Yoh 3:15
Yoh 5:24
1Pe 1:9
1Yo 5:13

Safu ya 2

SURA 21
a Yoh 11:16
Yoh 20:24
b Yoh 1:45
c Mt 4:21
d Lu 5:5
e Lu 24:16
Yoh 20:14
f Lu 5:4
g Lu 5:6
h Yoh 13:23
Yoh 19:26
Yoh 20:2
i Mt 14:29
j 1Fa 19:6

samaki mliowavua sasa hivi."
11 Kwa hiyo, Simoni Petro
akapanda ndani na kuuvuta
wavu kwenye nchi kavu ukiwa umejaa samaki wakubwa
153. Lakini ijapokuwa kuli-
kuwako wengi sana wavu ha-
ukupasuka. **12** Yesu akawaa-
mbia: "Njooni, mpate kiamsha-
kinywa chenu."[a] Hakuna hata
mmoja wa wanafunzi aliyeku-
wa na moyo wa kumuuliza:
"Wewe ni nani?" kwa sababu
walijua ni Bwana. **13** Yesu
akaja, akachukua mkate na ku-
wapa,[b] na samaki vivyo hivyo.
14 Sasa hii ilikuwa ni mara ya
tatu[c] ambayo Yesu aliwatokea
wanafunzi baada ya kufufuliwa
kwake kutoka kwa wafu.

15 Basi, walipokuwa wame-
pata kiamsha-kinywa, Yesu aka-
mwambia Simoni Petro: "Simo-
ni mwana wa Yohana, je, unani-
penda kuliko hawa?"[d] Akamwa-
mbia: "Ndiyo, Bwana, unajua
ninakupenda."[e] Akamwambia:
"Lisha wana-kondoo wangu."[f]
16 Tena akamwambia, mara
ya pili: "Simoni mwana wa Yo-
hana, je, unanipenda?"[g] Aka-
mwambia: "Ndiyo, Bwana, una-
jua ninakupenda." Akamwa-
mbia: "Chunga kondoo wangu
wadogo."[h] **17** Akamwambia
mara ya tatu: "Simoni mwa-
na wa Yohana, je, unanipe-
nda?" Petro akahuzunika kwa-
mba alimwambia mara ya tatu:
"Je, unanipenda?" Kwa hiyo
akamwambia: "Bwana, wewe
unajua mambo yote;[i] unajua
kwamba ninakupenda." Yesu
akamwambia: "Lisha kondoo
wangu wadogo.[j] **18** Kwa kwe-
li kabisa ninakuambia, Ulipo-
kuwa kijana, ulikuwa ukijifu-
nga kiuno na kutembea huku
na huku kokote ulikotaka. La-
kini utakapozeeka utanyoosha
mikono yako na mtu mwingi-
ne atakufunga kiuno[a] na ku-
kupeleka usikotaka wewe."[b]
19 Hilo alisema ili kutoa isha-
ra ni kwa kifo[c] cha namna gani
yeye angemtukuza Mungu.[d]
Kwa hiyo, alipokuwa amese-
ma hayo, akamwambia: "Ende-
lea kunifuata."[e]

20 Petro alipogeuka, ali-
mwona mwanafunzi ambaye
Yesu alikuwa akimpenda,[f] aki-
fuata, yule ambaye kwenye mlo
wa jioni alikuwa pia ameege-
mea nyuma kifuani pake aka-
sema: "Bwana, ni nani anaye-
kusaliti?" **21** Basi, alipomwo-
na, Petro akamwambia Yesu:
"Bwana, mtu huyu atafanya
nini?" **22** Yesu akamwambia:
"Ikiwa ni mapenzi yangu akae
mpaka nije,[g] hilo linakuhusu
nini wewe? Wewe endelea kuni-
fuata mimi." **23** Kwa sababu
hiyo, maneno hayo yakaenea
kati ya akina ndugu, kwamba
mwanafunzi huyo hangekufa.
Hata hivyo, Yesu hakumwa-
mbia kwamba hangekufa, bali:
"Ikiwa ni mapenzi yangu akae[h]
mpaka nije, hilo linakuhusu
nini wewe?"

24 Huyo ndiye mwanafunzi[i]
ambaye anatoa ushahidi juu ya
mambo haya na ambaye aliyaa-
ndika mambo haya, na sisi tu-
najua kwamba ushahidi anao-
toa ni wa kweli.[j]

25 Kwa kweli, kuna mambo
mengine mengi pia aliyofanya
Yesu, ambayo, kama yangea-
ndikwa kirefu, nadhani uli-
mwengu wenyewe haungewe-
za kuwa na nafasi ya kuviweka
vitabu vya kukunjwa ambavyo
vingeandikwa.[k]

SURA 21

a Mdo 10:41
b Lu 24:30
c Yoh 20:19
Yoh 20:26
d Yoh 21:12
e Mt 26:33
Yoh 17:26
f Lu 22:32
Mdo 20:28
1Pe 5:2
g Yoh 14:21
h Zb 95:7
Mt 10:6
Mdo 1:15
Mdo 2:14
Ebr 13:20
1Pe 2:25
i Mk 2:8
Yoh 2:24
Yoh 2:25
Yoh 16:30
j Yoh 10:3
Yoh 10:16

Safu ya 2

a Mdo 21:11
b Mdo 12:3
c 2Pe 1:14
d Flp 1:20
e Mt 19:28
Yoh 12:26
Ufu 14:4
f Yoh 13:23
Yoh 20:2
g Mt 16:27
Mt 25:31
1Ko 4:5
Ufu 1:10
Ufu 22:20
h Ufu 1:1
Ufu 1:9
i Yoh 13:23
Yoh 19:26
Yoh 20:2
Yoh 21:7
j Yoh 19:35
3Yo 12
k Yoh 20:30

MATENDO YA MITUME

1 Lile simulizi la kwanza, Ee
Theofilo,[a] nilitunga juu ya
mambo yote ambayo Yesu ali-
anza kufanya na pia kufundi-
sha,[b] **2** mpaka siku aliyochu-
kuliwa juu,[c] alipokuwa ame-
toa amri kupitia roho takati-
fu kwa mitume aliowachagua.[d]
3 Kwa uthibitisho mwingi ulio
hakika, alijionyesha kwa hawa
pia akiwa hai alipokuwa ame-
teseka,[e] nao wakamwona kwa
siku 40 na kusema juu ya ufa-
lme wa Mungu.[f] **4** Naye ali-
pokuwa akikutana pamoja nao
aliwapa maagizo haya: "Msi-
ondoke Yerusalemu,[g] bali ende-
leeni kungojea kile ambacho
Baba ameahidi,[h] ambacho mli-
sikia juu yake kutoka kwa-
ngu; **5** kwa sababu Yohana,
kwa kweli, alibatiza kwa maji,
lakini ninyi mtabatizwa kwa
roho takatifu[i] siku chache baa-
daye."

6 Basi, walipokuwa wame-
kusanyika, wakaanza kumu-
uliza: "Bwana, je, unarudishia
Israeli ufalme[j] wakati huu?"
7 Akawaambia: "Si juu yenu
kujua nyakati au majira[k]
ambayo Baba ameweka kati-
ka mamlaka yake mwenyewe;[l]
8 lakini mtapokea nguvu[m] wa-
kati roho takatifu itakapofi-
ka juu yenu, nanyi mtakuwa
mashahidi[n] wangu katika Ye-
rusalemu[o] na pia katika Yudea
yote na Samaria[p] na mpaka se-
hemu ya mbali zaidi ya dunia."[q]
9 Na alipokuwa amesema ma-
mbo hayo, huku walipokuwa
wakitazama, akainuliwa[r] na
wingu likamchukua juu kuto-
ka machoni pao.[a] **10** Nao wa-
lipokuwa wakitazama angani
alipokuwa ameondoka na kwe-
nda,[b] pia, tazama! wanaume wa-
wili wenye mavazi meupe[c] wa-
kasimama kando yao, **11** nao
wakasema: "Wanaume wa Ga-
lilaya, kwa nini mnasimama
mkitazama angani? Yesu huyu
aliyepokewa juu angani kuto-
ka kwenu atakuja vivyo hivyo[d]
kama vile ambavyo mmemwo-
na akienda angani."

12 Ndipo wakarudi[e] Yerusa-
lemu kutoka katika mlima una-
oitwa Mlima wa Mizeituni, ulio
karibu na Yerusalemu, ukiwa
ni umbali wa safari ya siku
ya sabato.[f] **13** Kwa hiyo, wa-
lipokuwa wameingia, wakapa-
nda na kuingia katika chu-
mba cha juu,[g] ambamo waliku-
wa wakikaa, Petro vilevile Yo-
hana na Yakobo na Andrea,
Filipo na Tomasi, Bartholoma-
yo na Mathayo, Yakobo mwa-
na wa Alfayo na Simoni mwe-
nye bidii, na Yuda mwana wa
Yakobo.[h] **14** Kwa umoja wote
hawa walikuwa wakidumu ka-
tika sala,[i] pamoja na wanawake[j]
fulani na Maria mama ya Yesu
na pamoja na ndugu zake.[k]

15 Sasa katika siku hizo Pe-
tro akasimama katikati ya
akina ndugu na kusema (watu
wote pamoja katika ule umati
walikuwa karibu 120): **16** "Wa-
naume, akina ndugu, ilikuwa la-
zima andiko litimizwe,[l] ambalo
roho takatifu[m] ilisema kimbele
kwa kinywa cha Daudi kumhu-
su Yuda,[n] aliyekuwa kiongozi
kwa wale waliomkamata Yesu,[o]

SURA 1

a Lu 1:3
b Lu 3:23
c Efe 4:10
1Ti 3:16
1Pe 3:22
d Mt 28:20
Lu 6:13
Yoh 15:16
e Mt 28:9
Yoh 20:19
1Ko 15:6
f Lu 24:27
g Lu 24:49
h Yoh 14:16
Mdo 2:33
i Yoe 2:28
Mt 3:11
Mk 1:8
j Isa 1:26
Da 7:27
Mik 4:8
Lu 19:11
Lu 24:21
k Da 2:21
Da 7:25
Lu 21:24
l Kum 29:29
Mt 24:36
m Mdo 4:33
n Isa 43:10
Lu 24:48
Yoh 15:27
o Mdo 5:28
p Mdo 8:14
q Kol 1:23
r Yoh 6:62

Safu ya 2

a Lu 24:51
b 1Pe 3:22
c Mt 28:3
Lu 24:4
d Da 7:13
Mt 26:64
Ufu 1:7
e Lu 24:52
f Kut 16:29
Yoh 11:18
g Mdo 9:37
h Mt 10:2
Mk 3:16
i Kol 4:2
1Th 5:17
j Lu 23:49
k Mt 13:55
Yoh 7:5
Ga 1:19
l Yoh 13:18
m Mk 12:36
n Zb 41:9
Zb 55:12
Lu 22:47
o Yoh 18:3

17 kwa sababu alikuwa amehesabiwa kati yetu[a] naye alipata fungu katika huduma hii.[b]
18 (Kwa hiyo, mtu huyo alinunua[c] shamba kwa mshahara wa ukosefu wa uadilifu,[d] akaanguka kichwa kwanza[e] akapasuka kwa kelele katikati na matumbo yake yote yakamwagika nje. **19** Pia ikajulikana kwa wakaaji wote wa Yerusalemu, hivi kwamba shamba hilo likaitwa katika lugha yao *Akeldama,* yaani, Shamba la Damu.)
20 Kwa maana imeandikwa katika kitabu cha Zaburi, 'Makao yake yawe na ukiwa, na pasiwe na mkaaji humo,'[f] na, 'Cheo chake cha uangalizi mtu mwingine na akichukue.'[g] **21** Kwa hiyo ni lazima kwamba kati ya wanaume waliokusanyika pamoja nasi wakati wote ambao Bwana Yesu aliingia na kutoka kati yetu,[h] **22** kuanzia na ubatizo wake uliofanywa na Yohana[i] mpaka siku aliyopokewa juu kutoka kwetu,[j] mmoja wa watu hao anapaswa kuwa shahidi pamoja nasi juu ya ufufuo wake."[k]

23 Kwa hiyo wakasimamisha wawili, Yosefu anayeitwa Barsaba, aliyeitwa pia Yusto, na Mathia. **24** Nao wakasali na kusema: "Wewe, Ee Yehova, ambaye unajua mioyo ya wote,[l] onyesha ni nani kati ya watu hawa wawili ambaye umemchagua, **25** achukue mahali pa huduma na utume[m] huu, ambao kutoka kwake Yuda alikengeuka ili kwenda mahali pake mwenyewe." **26** Kwa hiyo wakawapigia kura,[n] na kura ikamwangukia Mathia; naye akahesabiwa pamoja na wale mitume kumi na mmoja.[o]

SURA 1
a Lu 6:16
Yoh 6:71
b Mt 10:4
c Mt 27:5
d Zek 11:12
Mt 26:15
2Pe 2:15
e Zb 55:23
f Zb 69:25
g Zb 109:8
1Ti 3:1
h Yoh 15:27
i Mt 3:13
Mdo 10:37
j Lu 24:51
k Mt 28:6
Mk 16:6
Mdo 1:9
l 1Sa 16:7
1Nya 28:9
Yer 11:20
Mdo 15:8
m Yoh 6:70
n Met 16:33
o Mt 28:16

Safu ya 2

SURA 2
a Law 23:16
Kum 16:9
b Mdo 4:31
c Mk 1:8
d Yoh 14:26
Mdo 6:3
1Pe 1:12
e Mdo 10:46
1Ko 12:10
f Kut 23:17
g Mdo 22:12
h Mk 14:70
Mdo 1:11
i 2Fa 17:6
j Da 8:2
k Mt 24:16
Mk 1:5
l 1Pe 1:1
m Mdo 18:2
n Mdo 13:1
1Pe 1:1
o Mdo 16:6
Mdo 18:23
p Mdo 13:13
Mdo 15:38
q Kut 12:48
Isa 56:6
r Tit 1:12
s 2Nya 17:11

2 Basi siku ya sherehe ya Pentekoste[a] ilipokuwa ikiendelea walikuwa wote pamoja mahali pale pale, **2** na ghafula kukatokea kutoka mbinguni kelele kama ile ya upepo wenye nguvu unaovuma, nao ukaijaza nyumba yote ambamo walikuwa wameketi.[b] **3** Nao wakaona ndimi kama za moto,[c] nazo zikagawanyika huku na huku, na mmoja ukaketi juu ya kila mmoja wao, **4** nao wote wakajazwa roho takatifu[d] wakaanza kusema katika lugha[e] tofauti, kama vile roho ilivyokuwa ikiwawezesha kusema.

5 Ikawa kwamba, kulikuwa na Wayahudi[f] wakikaa katika Yerusalemu, watu wenye kumheshimu Mungu,[g] kutoka kila taifa kati ya yale yaliyo chini ya mbingu. **6** Kwa hiyo, mvumo huo ulipotokea, umati ukaja pamoja nao ukashikwa na bumbuazi, kwa sababu kila mmoja aliwasikia wakisema katika lugha yake mwenyewe. **7** Kwa kweli, walishangaa na kuanza kustaajabu na kusema: "Tazama, wote hawa wanaosema ni Wagalilaya,[h] sivyo? **8** Hata hivyo, imewezekanaje kwamba sisi, kila mmoja wetu, tunasikia lugha yake mwenyewe tuliyozaliwa nayo? **9** Waparthi na Wamedi[i] na Waelami,[j] na wakaaji wa Mesopotamia, na Yudea[k] na Kapadokia,[l] Ponto[m] na wilaya ya Asia,[n] **10** na Frigia[o] na Pamfilia,[p] Misri, na sehemu za Libya, ambayo ni kuelekea Kirene, na wakaaji wa muda wa kutoka Roma, Wayahudi na pia wageuzwa-imani,[q] **11** Wakreter[r] na Waarabu,[s] tunawasikia wakisema katika lugha zetu juu ya mambo makuu ya Mungu."

12 Ndiyo, wote wakashangaa
na kustaajabu, wakiambiana:
"Jambo hili linamaanisha nini?"
13 Hata hivyo, watu tofauti
waliwadhihaki na kuanza kusema: "Wamejaa divai tamu."[a]

14 Lakini Petro akasimama
pamoja na wale kumi na mmoja[b] na kupaaza sauti yake na
kuwaambia hivi: "Watu wa Yudea nanyi nyote wakaaji wa Yerusalemu,[c] acheni hili lijulikane
kwenu nanyi tegeni sikio msikie maneno yangu. **15** Kwa
kweli, watu hawa hawakulewa,[d] kama mnavyofikiri, kwa
maana ni saa tatu ya mchana. **16** Badala yake, hili ndilo lililosemwa kupitia nabii Yoeli, **17** '"Na katika siku za
mwisho," Mungu asema, "Nitaimimina sehemu ya roho yangu[e] juu ya kila namna ya
mwili, nao wana wenu na binti zenu watatoa unabii nao wanaume wenu vijana wataona
maono na wazee wenu watao-
ta ndoto;[f] **18** na hata juu ya
watumwa wangu na juu ya wajakazi wangu nitaimimina sehemu ya roho yangu katika
siku hizo, nao watatoa unabii.[g]
19 Nami nitatoa maajabu mbinguni juu na ishara duniani
chini, damu na moto na ukungu wa moshi;[h] **20** jua[i] litageuzwa kuwa giza na mwezi kuwa
damu kabla ya kufika kwa ile
siku ya Yehova iliyo kuu na yenye fahari.[j] **21** Na kila mtu
anayeliitia jina la Yehova ataokolewa." '[k]

22 "Watu wa Israeli, sikieni
maneno haya: Yesu Mnazareti,[l]
mwanamume aliyeonyeshwa
hadharani na Mungu kwenu
kupitia kazi zenye nguvu[m]
na mambo ya ajabu na ishara

SURA 2

a 1Sa 1:14
b Mt 28:16
c Mdo 7:2
Mdo 22:1
d Mdo 26:25
1Th 5:7
e Isa 44:3
Eze 36:27
Zek 12:10
f Yoe 2:28
g Hes 11:29
Yoe 2:29
Mdo 21:4
1Ko 12:10
h Yoe 2:30
i Mt 24:29
j Yoe 2:31
Mk 13:24
k Yoe 2:32
Ro 10:13
l Mt 2:23
m Lu 24:19
Yoh 5:36

Safu ya 2

a Yoh 14:10
Ebr 2:4
b Lu 24:44
Yoh 19:11
Mdo 4:28
1Pe 1:20
c Lu 23:33
Mdo 5:30
Mdo 7:52
d Zb 16:10
Mdo 3:15
Ro 4:24
1Ko 6:14
Kol 2:12
Ebr 13:20
e Zb 9:13
f Yoh 10:18
g Zb 16:8
h Zb 16:9
i Zb 16:10
Mdo 13:35
j Zb 16:11
k 1Fa 2:10
Mdo 13:36
l 2Sa 7:12
Zb 89:4
Zb 132:11

ambazo Mungu alifanya kupitia kwake katikati yenu,[a] kama
vile ninyi wenyewe mnavyojua,
23 mwanamume huyu, kama
aliyetolewa kwa shauri lililoamuliwa na kwa ujuzi wa kimbele wa Mungu,[b] mlimfunga
kwenye mti kwa mkono wa
waasi-sheria na kumwondolea
mbali.[c] **24** Lakini Mungu alimfufua[d] kwa kuyafungua maumivu makali ya kifo,[e] kwa sababu haikuwezekana kiendelee kumshika.[f] **25** Kwa maana Daudi anasema juu yake,
'Yehova alikuwa mbele ya macho yangu daima; kwa sababu yuko upande wa mkono wangu wa kuume ili nisipate kutikiswa kamwe.[g] **26** Kwa ajili
ya hilo moyo wangu ulichangamka na ulimi wangu ukashangilia sana. Zaidi ya hayo,
hata mwili wangu utakaa katika tumaini;[h] **27** kwa sababu hutaiacha nafsi yangu katika Kaburi,* wala hutamruhusu mshikamanifu wako aone
uharibifu.[i] **28** Umefanya njia
za uzima zijulikane kwangu,
utanijaza uchangamfu mwingi
kwa uso wako.'[j]

29 "Wanaume, akina ndugu,
inaruhusika kusema nanyi kwa
uhuru wa kusema juu ya Daudi yule kichwa cha familia, kwamba alikufa[k] na pia akazikwa
na kaburi lake liko katikati
yetu mpaka leo hii. **30** Kwa
hiyo, kwa sababu alikuwa nabii na alijua kwamba Mungu alikuwa amemwapia kwa kiapo
kwamba angemketisha mmoja
kutoka kati ya uzao wa viuno vyake juu ya kiti chake cha
ufalme,[l] **31** aliona kimbele na

Mdo 2:27* Hadesi. Tazama Nyongeza 4.

kusema kuhusu ufufuo wa Kristo, kwamba hakuachwa katika Kaburi* wala mwili wake haukuona uharibifu.[a] **32** Yesu huyo Mungu alimfufua, uhakika ambao sisi sote ni mashahidi.[b] **33** Kwa hiyo kwa sababu aliinuliwa kwenye mkono wa kuume wa Mungu[c] na kupokea roho takatifu iliyoahidiwa kutoka kwa Baba,[d] amemimina hiki ambacho ninyi mnakiona na kukisikia. **34** Kwa kweli Daudi hakupanda mbinguni,[e] bali yeye mwenyewe anasema, 'Yehova alimwambia Bwana wangu: "Keti kwenye mkono wangu wa kuume,[f] **35** mpaka niwaweke adui zako kuwa kiti cha miguu yako."'[g] **36** Kwa hiyo acha nyumba yote ya Israeli ijue kwa hakika kwamba Mungu alimfanya Bwana[h] na pia Kristo, Yesu huyu ambaye ninyi mlimtundika mtini."[i]

37 Basi waliposikia hilo walichomwa moyoni,[j] nao wakamwambia Petro na wale mitume wengine: "Wanaume, akina ndugu, tufanye nini?"[k] **38** Petro akawaambia: "Tubuni,[l] na acheni kila mmoja wenu abatizwe[m] katika jina[n] la Yesu Kristo kwa msamaha[o] wa dhambi zenu, nanyi mtapokea zawadi ya bure[p] ya roho takatifu. **39** Kwa maana ahadi[q] ni kwenu na kwa watoto wenu na kwa wale wote walio mbali,[r] wengi kadiri ambayo Yehova Mungu wetu huenda akawaita kwake."[s] **40** Na kwa maneno mengine mengi akatoa ushahidi kamili na kuendelea kuwahimiza, akisema: "Okoleweni kutoka katika kizazi hiki kilicho kombo."[a] **41** Kwa hiyo wale waliokubali neno lake kwa ukunjufu wa moyo wakabatizwa,[b] na katika siku hiyo nafsi karibu elfu tatu zikaongezwa.[c] **42** Nao wakaendelea kujitoa wenyewe kwa fundisho la mitume na kushirikiana,[d] katika kula milo[e] na katika sala.[f]

43 Kwa kweli, woga ukaanza kuwa juu ya kila nafsi, na mambo mengi ya ajabu na ishara nyingi zikaanza kutukia kupitia mitume.[g] **44** Wale wote waliopata kuwa waamini walikuwa pamoja katika kuwa na mambo yote kwa ushirika,[h] **45** nao wakaanza kuuza miliki na mali zao[i] na kuwagawia wote mapato hayo, kulingana na vile yeyote alivyokuwa na uhitaji.[j] **46** Na siku baada ya siku walikuwa wakihudhuria daima kwenye hekalu kwa umoja,[k] nao walikula milo yao katika nyumba za faragha na kushiriki chakula kwa shangwe[l] kuu na weupe wa moyo, **47** wakimsifu Mungu na kupata kibali kwa watu wote.[m] Wakati uleule Yehova akaendelea kuongezea[n] kwao kila siku wale waliokuwa wakiokolewa.[o]

3 Basi Petro na Yohana walikuwa wakipanda kwenda hekaluni kwa ajili ya saa ya sala, saa tisa,[p] **2** na mwanamume fulani aliyekuwa kilema tangu alipokuwa katika tumbo la uzazi la mama yake[q] alikuwa akibebwa, nao walikuwa wakimweka kila siku karibu na mlango wa hekalu ulioitwa Mzuri,[r] ili kuomba zawadi za rehema kutoka kwa wale waliokuwa wakiingia katika hekalu.[s] **3** Alipowaona Petro na Yohana wakiwa karibu kuingia ndani ya hekalu akaa-

SURA 2

a Zb 16:10 Mdo 13:35 Mdo 13:37
b Lu 24:48 Mdo 1:8 Mdo 3:15
c Ro 8:34 Flp 2:9 1Pe 3:22
d Yoh 14:26 Mdo 1:4
e Yoh 3:13
f Zb 110:1
g Mwa 3:15 Lu 20:43 1Ko 15:25 Ebr 10:13
h Mt 28:18 Yoh 3:35 Mdo 5:31
i Yoh 19:6 Mdo 4:10
j 2Sa 24:10 Zb 73:21
k Lu 3:10 Mdo 16:30
l Lu 24:47 Mdo 17:30 Mdo 26:20
m Mt 28:19
n Flp 2:9 Ufu 19:16
o Isa 44:22 Mt 26:28 Efe 1:7
p Mdo 8:20
q Yoe 2:28
r Isa 57:19 Efe 2:17
s Yoe 2:32

Safu ya 2

a Kum 32:5 Zb 78:8 Ga 1:4 Flp 2:15
b Mdo 8:12 Mdo 18:8
c Isa 60:22 Mdo 4:4 Mdo 5:14
d Flp 1:5
e Mdo 2:46
f Mdo 1:14
g Mdo 5:12 Mdo 19:17
h Mdo 4:32
i Mt 19:21
j Isa 58:7 Mdo 4:34
k Lu 24:53
l Mhu 9:7
m Ro 14:18
n Zb 115:14 1Ko 3:7
o Mdo 5:14 Mdo 11:21 Mdo 11:24

SURA 3

p Mdo 10:30
q Yoh 9:1 Mdo 14:8
r Mdo 3:10
s Yoh 9:8

Mdo 2:31* Hadesi. Tazama Nyongeza 4.

nza kuomba apate zawadi za rehema.[a] **4** Lakini Petro, pamoja na Yohana, wakamtazama[b] na kusema: “Tuangalie sisi.” **5** Kwa hiyo akawaangalia, akitarajia kupata kitu fulani kutoka kwao. **6** Hata hivyo, Petro akasema: “Fedha na dhahabu sina, lakini kile nilicho nacho ndicho ninachokupa:[c] Katika jina la Yesu Kristo Mnazareti,[d] tembea!”[e] **7** Ndipo akamshika mkono wa kuume na kumwinua.[f] Papo hapo nyayo za miguu yake na vifundo vya miguu yake vikafanywa imara;[g] **8** naye akaruka juu,[h] akasimama na kuanza kutembea, kisha akaingia pamoja nao katika hekalu,[i] akitembea na kuruka-ruka na kumsifu Mungu. **9** Na watu wote[j] wakamwona akitembea na kumsifu Mungu. **10** Zaidi ya hayo, wakaanza kumtambua, kwamba huyu ndiye mtu aliyekuwa akiketi kwa ajili ya zawadi za rehema penye Lango Zuri[k] la hekalu, nao wakajawa na mshangao na shangwe[l] kwa sababu ya jambo lililokuwa limetukia kwake.

11 Basi, kwa kuwa mtu huyo alikuwa akiwashikilia Petro na Yohana, watu wote waliwakimbilia pamoja kwenye eneo lililoitwa mistari ya nguzo za Sulemani,[m] wakiwa wamepotewa na akili kwa sababu ya mshangao. **12** Petro alipoona jambo hilo, akawaambia watu hao: “Watu wa Israeli, kwa nini mnastaajabu juu ya hili, au kwa nini mnatutazama kana kwamba tumemfanya atembee kwa nguvu za kibinafsi au kwa ujitoaji-kimungu?[n] **13** Mungu wa Abrahamu na wa Isaka na wa Yakobo,[o] Mungu wa mababu zetu, amemtukuza[a] Mtumishi[b] wake, Yesu, ambaye ninyi mlimpeleka[c] na kumkana mbele ya uso wa Pilato, alipokuwa ameamua kumfungua.[d] **14** Ndiyo, ninyi mlimkana huyo aliye mtakatifu na mwadilifu,[e] nanyi mkaomba mpewe kwa hiari mwanamume, muuaji,[f] **15** lakini mlimuua Wakili Mkuu wa uzima.[g] Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, uhakika ambao sisi ni mashahidi[h] wake. **16** Kwa sababu hiyo, kwa imani yetu katika jina lake, jina lake limemfanya awe mwenye nguvu mtu huyu ambaye mnamwona na kumjua, na imani kupitia kwake imempa mtu huyu afya hii kamili mbele ya macho yenu nyote. **17** Na sasa, akina ndugu, ninajua kwamba mlitenda kwa kutojua,[i] kama vile watawala[j] wenu pia walivyotenda. **18** Lakini katika njia hiyo Mungu ametimiza mambo aliyotangaza kimbele kupitia kinywa cha manabii wote, kwamba Kristo wake angeteseka.[k]

19 “Kwa hiyo, tubuni[l] na mgeuke[m] ili dhambi zenu zipate kufutwa,[n] ili majira ya kuburudisha[o] yapate kuja kutoka kwa uso wa Yehova **20** na kwamba apate kumtuma Kristo aliyewekwa rasmi kwa ajili yenu, Yesu, **21** ambaye mbingu, kwa kweli,[p] lazima imweke ndani yake mpaka nyakati za kurudishwa[q] kwa mambo yote ambayo Mungu alisema kupitia kinywa cha manabii[r] wake watakatifu wa nyakati za kale. **22** Kwa kweli, Musa alisema, ‘Yehova Mungu atawainulia kutoka kati ya ndugu zenu nabii kama mimi.[s] Msikilizeni huyo

SURA 3

a Lu 11:41
b Mdo 14:9
c 2Ko 6:10
d Mt 2:23
Mdo 4:10
e Mdo 3:16
f Mt 9:25
Lu 6:6
g Mt 8:15
Yoh 5:8
Mdo 9:34
Mdo 14:10
h Isa 35:6
i Yoh 5:14
j Mdo 4:21
k Yoh 9:8
Mdo 3:2
l Mk 5:42
m Yoh 10:23
Mdo 5:12
n 2Ko 3:5
o Kut 3:6
Mt 22:32

Safu ya 2

a Yoh 7:39
Flp 2:9
b Isa 52:13
Isa 53:11
c Mdo 2:23
Mdo 5:30
d Mt 27:21
Lu 23:14
e 1Yo 2:1
f Mt 27:20
Lu 23:18
g Mdo 5:31
Ebr 2:10
h Lu 24:48
Mdo 1:8
Mdo 2:32
i Lu 23:34
Yoh 16:3
1Ti 1:13
j 1Ko 2:8
k Zb 22:16
Zb 118:22
Isa 50:6
Isa 53:8
Da 9:26
Lu 22:15
l Mdo 2:38
m Eze 33:11
Efe 4:22
1Pe 4:3
n Eze 33:16
1Yo 1:7
o Isa 28:12
p Zb 110:1
q Mt 17:11
r Isa 1:26
s Kum 18:15
Kum 34:10

kulingana na mambo yote anayowaambia ninyi.[a] **23** Kwa kweli, nafsi yoyote isiyomsikiliza Nabii huyo itaangamizwa kutoka kati ya watu.'[b] **24** Na kwa kweli, manabii wote tangu Samweli na kuendelea na wale waliofuata, wengi kadiri ambavyo wamesema, wamezitangaza waziwazi pia siku hizi.[c] **25** Ninyi ndio wana[d] wa manabii na wa agano ambalo Mungu aliagana pamoja na mababu zenu, akimwambia Abrahamu, 'Na katika uzao wako familia zote za dunia zitabarikiwa.'[e] **26** Baada ya kumwinua Mtumishi wake, Mungu alimtuma kwenu kwanza[f] ili kuwabariki ninyi kwa kugeuzia mbali kila mmoja kutoka kwenye matendo yenu maovu."

4 Sasa hao wawili walipokuwa wakisema na watu, wakuu wa makuhani na kapteni wa hekalu[g] na Masadukayo[h] wakawajia, **2** wakiwa wameudhika kwa sababu walikuwa wakiwafundisha watu na walikuwa wakiutangaza waziwazi ufufuo kutoka kwa wafu kwa kisa cha Yesu;[i] **3** nao wakawashika na kuwaweka katika kizuizi mpaka siku iliyofuata,[j] kwa maana tayari ilikuwa jioni. **4** Hata hivyo, wengi kati ya wale waliokuwa wamesikiliza maneno hayo wakaamini,[k] na hesabu ya wanaume ikawa karibu elfu tano.[l]

5 Siku iliyofuata kukawa na mkutano wa watawala wao na wanaume wazee na waandishi katika Yerusalemu[m] **6** (pia Anasi[n] mkuu wa makuhani na Kayafa[o] na Yohana na Aleksanda na wengi waliokuwa watu wa jamaa ya huyo mkuu wa makuhani), **7** nao wakawasimamisha katikati yao na kuanza kuuliza: "Mlifanya jambo hilo kwa nguvu gani au katika jina la nani?"[a] **8** Ndipo Petro, akiwa amejazwa roho takatifu,[b] akawaambia:

"Watawala wa watu na wanaume wazee, **9** ikiwa leo sisi tunahojiwa, juu ya msingi wa tendo jema kwa mtu mwenye kuugua,[c] kuhusu ni nani amemponya mtu huyu, **10** acheni ijulikane kwenu nyote na kwa watu wote wa Israeli, kwamba katika jina la Yesu Kristo Mnazareti,[d] ambaye mlimtundika mtini[e] lakini ambaye Mungu alimfufua kutoka kwa wafu,[f] kupitia kwake, mtu huyu anasimama hapa akiwa na afya mbele yenu. **11** Hilo ndilo 'jiwe ambalo ninyi wajenzi mlilitendea kana kwamba si la maana ambalo limekuwa jiwe kuu la pembeni.'[g] **12** Zaidi ya hayo, hakuna wokovu katika mwingine yeyote, kwa maana hakuna jina[h] lingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu ambalo kupitia hilo lazima sisi tupate kuokolewa."[i]

13 Sasa walipoona maneno ya waziwazi ya Petro na Yohana, na kufahamu kwamba walikuwa watu wasio na elimu na wa kawaida tu,[j] wakaanza kustaajabu. Nao wakaanza kutambua juu yao kwamba walikuwa pamoja na Yesu;[k] **14** nao walipokuwa wakitazama mtu aliyekuwa ameponywa akiwa amesimama pamoja nao,[l] hawakuwa na jambo la kukanusha.[m] **15** Kwa hiyo wakawaamuru waende nje ya jumba la Sanhedrini, nao wakaanza kushauriana, **16** wakisema: "Tutafanya

SURA 3
a Kum 18:18
Mdo 7:37
b Kum 18:19
c Lu 24:27
Mdo 10:43
d Ro 9:4
e Mwa 22:18
Ga 3:8
f Mdo 13:46
Ro 1:16

SURA 4
g Lu 22:4
h Mdo 23:8
i Mdo 4:33
Mdo 17:18
j Lu 21:12
k 1Ti 3:16
l Mdo 2:41
Mdo 6:7
m Mk 13:9
n Lu 3:2
Yoh 18:13
o Mt 26:57
Lu 3:2
Yoh 11:49

Safu ya 2
a Mt 21:23
Mk 11:28
Lu 20:2
b Mdo 7:55
c Mdo 3:7
d Mt 2:23
Mdo 3:6
e Mdo 2:36
f Mdo 2:24
Mdo 5:30
g Zb 118:22
Isa 28:16
Mt 21:42
1Pe 2:7
h Mt 1:21
Mdo 10:43
Flp 2:9
i Yoh 1:12
Yoh 14:6
1Ti 2:5
j Mt 11:25
1Ko 1:27
k Yoh 7:15
l Mdo 3:11
m Lu 21:15

nini na watu hawa?[a] Kwa sababu, kwa kweli, ishara kuu imetukia kupitia kwao, ambayo ni wazi kwa wakaaji wote wa Yerusalemu;[b] nasi hatuwezi kuikana. **17** Hata hivyo, ili isipate kusambazwa zaidi kotekote kati ya watu, acheni tuwaambie kwa vitisho wasiseme tena kamwe na mtu yeyote juu ya msingi wa jina hilo."[c]

18 Ndipo wakawaita na kuwaamuru wasiseme wala kufundisha popote juu ya msingi wa jina la Yesu. **19** Lakini Petro na Yohana wakajibu wakawaambia: "Kama ni jambo la uadilifu mbele za macho ya Mungu kuwasikiliza ninyi badala ya Mungu, hukumuni ninyi wenyewe. **20** Lakini sisi hatuwezi kuacha kusema juu ya mambo ambayo tumeyaona na kuyasikia."[d] **21** Kwa hiyo, walipokuwa wamewatisha zaidi, wakawafungua, kwa kuwa hawakupata msingi wowote wa kuwaadhibu na kwa sababu ya watu,[e] kwa sababu wote walikuwa wakimtukuza Mungu juu ya jambo lililokuwa limetukia; **22** kwa maana mtu ambaye ishara hiyo ya kuponywa ilikuwa imetokea juu yake alikuwa na umri wa zaidi ya miaka 40.

23 Baada ya kufunguliwa wakaenda kwa watu wao[f] wenyewe na kuwaeleza mambo ambayo wakuu wa makuhani na wanaume wazee walikuwa wamewaambia. **24** Waliposikia hayo wakampaazia Mungu[g] sauti zao kwa umoja na kusema:

"Bwana Mwenye Enzi Kuu,[h] wewe Ndiye uliyefanya mbingu na dunia na bahari na vitu vyote vilivyomo,[i] **25** na ambaye kupitia roho takatifu ulisema kwa kinywa cha babu yetu Daudi,[a] mtumishi wako, 'Kwa nini mataifa yakawa yenye fujo na vikundi vya watu vikatafakari juu ya mambo matupu?[b] **26** Wafalme wa dunia walichukua msimamo wao nao watawala wakajikusanya pamoja kama mtu mmoja dhidi ya Yehova na dhidi ya mtiwa-mafuta wake.'[c] **27** Ijapokuwa hivyo, Herode na pia Pontio Pilato[d] pamoja na watu wa mataifa na pamoja na vikundi vya watu wa Israeli kwa kweli walikusanyika pamoja katika jiji hili dhidi ya mtumishi wako mtakatifu[e] Yesu, ambaye ulimtia mafuta,[f] **28** ili afanye mambo ambayo mkono wako na shauri viliagiza kimbele yatukie.[g] **29** Na sasa, Yehova, viangalie vitisho vyao,[h] na kuwawezesha watumwa wako kuendelea kusema neno lako kwa ujasiri wote,[i] **30** huku ukiunyoosha mkono wako ili kuponya na huku ishara[j] nyingi na mambo ya ajabu yakitukia kupitia jina[k] la mtumishi[l] wako mtakatifu Yesu."

31 Nao walipokuwa wameomba dua, mahali hapo walipokuwa wamekusanyika pamoja pakatikiswa;[m] nao wote wakajazwa roho takatifu[n] na wakawa wakisema neno la Mungu kwa ujasiri.[o]

32 Zaidi ya hayo, umati wa waliokuwa wameamini ulikuwa na moyo na nafsi moja,[p] na hakuna hata mmoja aliyekuwa akisema kwamba chochote kati ya vitu vilivyokuwa mali yake kilikuwa chake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote kwa ushirika.[q] **33** Pia, wakiwa na nguvu nyingi mitume

SURA 4

a Yoh 11:47
b Mdo 3:9
c Mdo 5:40
d Mdo 5:29
2Pe 1:16
e Lu 22:2
Mdo 5:26
f Mdo 12:12
g Zb 55:16
h Ufu 6:10
i Kut 20:11
Ne 9:6
Zb 146:6
Ufu 10:6

Safu ya 2

a 2Sa 23:2
b Zb 2:1
c Zb 2:2
d Lu 23:12
e Mdo 3:13
Ebr 7:26
f Zb 45:7
Mdo 10:38
g Isa 53:10
Lu 24:44
Mdo 2:23
1Pe 1:20
h Isa 37:17
i Isa 58:1
Mdo 19:8
j Mdo 2:43
Mdo 5:12
k Mdo 3:16
l Mdo 3:26
m Mdo 2:2
n Mdo 2:4
o 1Th 2:2
p Yoh 17:21
Flp 1:27
q Mdo 2:44

wakaendelea kutoa ushahidi
kuhusu ufufuo wa Bwana Yesu;[a]
na fadhili zisizostahiliwa kwa
kadiri kubwa zilikuwa juu yao
wote. **34** Kwa kweli, hapakuwa
hata mmoja mwenye uhi-
taji kati yao;[b] kwa maana wale
wote waliokuwa na mashamba
au nyumba walikuwa wakiviuza
na kuleta thamani za vitu
vilivyouzwa **35** nao walikuwa
wakiziweka miguuni pa mitume.[c]
Na kila mmoja alikuwa
akigawiwa,[d] kulingana na
uhitaji wake. **36** Kwa hiyo Yo-
sefu, ambaye mitume walikuwa
wakimwita Barnaba,[e] jina
ambalo linapotafsiriwa linama-
anisha Mwana wa Faraja, Mla-
wi, mzaliwa wa Kipro, **37** aki-
wa na sehemu ya shamba, akai-
uza na kuzileta pesa na kuziwe-
ka miguuni pa mitume.[f]

5 Hata hivyo, mwanamume
fulani, aliyeitwa Anania,
pamoja na Safira mke wake, ali-
uza mali **2** na kujiwekea kwa
siri kiasi fulani, mke wake pia
akiwa anajua jambo hilo,
naye akaleta sehemu fulani tu
na kuiweka miguuni pa mi-
tume.[g] **3** Lakini Petro aka-
sema: "Anania, kwa nini She-
tani[h] amekupa ujasiri wa kui-
danganya[i] roho takatifu[j] na
kujiwekea kwa siri kiasi fula-
ni cha bei ya shamba? **4** Ka-
bla ya kuuza je, haikuwa mali
yako, na baada ya kuuza je,
haikuendelea kuwa mikononi
mwako? Kwa nini ukakusudia
tendo kama hili katika moyo
wako? Umedanganya,[k] si wana-
damu, bali Mungu."[l] **5** Alipo-
sikia maneno hayo Anania aka-
anguka chini akakata pumzi.[m]
Na wote waliosikia juu ya hilo
wakaogopa[n] sana. **6** Lakini

SURA 4
a Mdo 1:22
Mdo 4:2
b Kum 15:4
Mdo 2:45
1Yo 3:17
c Mdo 5:2
d Mdo 6:1
e Mdo 11:22
Mdo 12:25
f Met 3:9
Lu 12:33

SURA 5
g Mdo 4:35
h Lu 22:3
i Zb 101:7
Zb 119:118
Efe 4:25
Kol 3:9
Ufu 21:8
j Hes 30:2
Mhu 5:4
Mdo 5:9
k Kum 23:23
l 1Sa 2:25
m 1Pe 4:17
n Mdo 2:43
Mdo 5:11

Safu ya 2
a Yoh 19:40
b Kut 17:2
Zb 95:9
Mt 4:7
Lu 4:12
1Ko 10:9
c Mdo 5:5
d Mdo 4:30
Mdo 6:8
Mdo 7:36
Mdo 14:3
Mdo 15:12
Ro 15:19
2Ko 12:12
e Yoh 10:23
Mdo 3:11
f Yoh 19:38
g Mdo 2:47
h Mdo 6:7

vijana wakasimama, wakamfu-
nga kwa vitambaa,[a] wakamtoa
nje, wakamzika.
7 Sasa baada ya muda wa ka-
ribu saa tatu mke wake aka-
ingia, bila kujua lililokuwa li-
metukia. **8** Petro akamwa-
mbia: "Niambie, je, ninyi wa-
wili mliliuza shamba kwa kiasi
hicho?" Akasema: "Ndiyo, kwa
kiasi hicho." **9** Kwa hiyo Pe-
tro akamwambia: "Kwa nini
mlikubaliana kati yenu wawi-
li kuijaribu[b] roho ya Yehova?
Tazama! Miguu ya wale walio-
mzika mume wako ipo mlango-
ni, nao watakubeba na kukutoa
nje." **10** Papo hapo akaangu-
ka chini miguuni pake akaka-
ta pumzi.[c] Wale vijana walipoi-
ngia wakamkuta amekufa, nao
wakamtoa nje wakamzika ka-
ndo ya mume wake. **11** Kwa
sababu hiyo kutaniko lote na
wote waliosikia juu ya mambo
haya wakaogopa sana.
12 Zaidi ya hayo, kupitia mi-
kono ya mitume ishara nyi-
ngi na mambo ya ajabu yaka-
endelea kutukia kati ya watu;[d]
nao wote walikuwa kwa umo-
ja katika eneo lenye mistari ya
nguzo za Sulemani.[e] **13** Kwe-
li, hakuna hata mmoja kati
ya wale wengine aliyekuwa na
moyo wa kujiunga nao;[f] hata hi-
vyo, watu walikuwa wakiwahi-
midi.[g] **14** Zaidi ya hayo, wa-
liomwamini Bwana wakaende-
lea kuongezeka, umati wa wa-
naume na pia wa wanawake;[h]
15 hivi kwamba wakawaleta
wagonjwa nje hata katika zile
njia pana na kuwalaza huko
juu ya vitanda na machela, ili,
wakati Petro anapopita hapo,
angalau kivuli chake kipate
kumwangukia mtu fulani kati

yao.[a] **16** Pia, umati kutoka
kwenye majiji yanayozunguka
Yerusalemu ukazidi kuja pa-
moja, ukiwa umewabeba wago-
njwa na wale wenye kutaabika
wakiwa na roho wachafu, nao
wote wakawa wakiponywa.

17 Lakini kuhani mkuu na
wote waliokuwa pamoja naye,
ile madhehebu ya Masaduka-
yo iliyokuwako wakati huo, wa-
kasimama na kujawa na wivu,[b]
18 nao wakawashika mitume
na kuwaweka katika kizuizi
cha watu wote.[c] **19** Lakini
wakati wa usiku malaika[d] wa
Yehova akaifungua milango ya
gereza,[e] akawatoa nje na ku-
sema: **20** "Nendeni, na, mki-
isha kusimama katika hekalu,
semeni na watu maneno yote
juu ya maisha haya."[f] **21** Ba-
ada ya kusikia hilo, wakaingia
hekaluni wakati wa mapamba-
zuko na kuanza kufundisha.

Basi kuhani mkuu na wale
walio pamoja naye walipofika,
wakaita pamoja Sanhedrini na
kusanyiko lote la wanaume wa-
zee wa wana wa Israeli,[g] nao wa-
kawatuma watu kwenye jela ili
waletwe. **22** Lakini wale ma-
ofisa walipofika huko hawaku-
wakuta gerezani. Kwa hiyo wa-
karudi na kuwaeleza, **23** wa-
kisema: "Tuliikuta jela imefu-
ngwa ikiwa na usalama wote
na walinzi wakiwa wamesima-
ma kwenye milango, lakini tu-
lipofungua hatukumkuta ye-
yote ndani." **24** Basi, wakati
kapteni wa hekalu na tena
wakuu wa makuhani waliposi-
kia maneno hayo, wakafadhai-
shwa sana na mambo hayo wasi-
jue mwisho wa jambo hilo unge-
kuwa nini.[h] **25** Lakini mtu fu-
lani akafika na kuwaambia:

SURA 5

a Mt 9:21
Mt 14:36
Mk 6:56
b Met 27:4
Mt 27:18
c Lu 21:12
Mdo 4:3
d Zb 34:7
Mdo 12:7
Ebr 1:14
e Mdo 16:26
f Yoh 6:68
g Mdo 4:5
h Mdo 4:1

Safu ya 2

a Mdo 4:20
b Mt 14:5
Lu 20:19
c Mdo 4:18
d Yoh 12:19
e Mt 27:25
Mdo 3:15
f 1Sa 15:22
Da 3:18
Yoh 14:15
Mdo 4:19
g Mdo 2:24
Mdo 13:30
h Mdo 2:23
Mdo 10:39
Ga 3:13
1Pe 2:24
i Mdo 3:15
j Mt 1:21
Ebr 2:10
k Mdo 2:33
Flp 2:9
l Mdo 2:38
m Isa 53:11
Lu 24:47
Mdo 10:43
Mdo 13:38
n Lu 24:48
Mdo 1:8
Mdo 1:22
o Yoh 15:26
p Mdo 7:54
q Mdo 22:3
r Mdo 4:15
s Mdo 2:22

"Tazameni! Wale watu mliowa-
weka gerezani wako hekaluni,
wakiwa wamesimama na ku-
wafundisha watu."[a] **26** Ndipo
kapteni akaenda zake pamoja
na maofisa wake na kuwaleta,
lakini bila kutumia jeuri, maa-
na waliogopa[b] kupigwa na watu
kwa mawe.

27 Kwa hiyo wakawaleta na
kuwasimamisha katika jumba
la Sanhedrini. Na kuhani mkuu
akawauliza **28** na kusema:
"Hakika tuliwaagiza[c] msiendelee
kufundisha juu ya msingi wa jina
hili, na bado, tazameni! mmeja-
za Yerusalemu fundisho lenu,[d]
nanyi mnaazimia kuileta damu[e]
ya mtu huyu juu yetu." **29** Pe-
tro na wale mitume wengine wa-
kajibu wakasema: "Lazima tu-
mtii Mungu kuwa mtawala ku-
liko wanadamu.[f] **30** Mungu wa
mababu zetu alimfufua[g] Yesu,
ambaye ninyi mlimuua, kwa ku-
mtundika mtini.[h] **31** Mungu
alimwinua huyo kuwa Wakili
Mkuu[i] na Mwokozi[j] kwenye mko-
no wake wa kuume,[k] ili kuwa-
pa Israeli toba[l] na msamaha wa
dhambi.[m] **32** Nasi ni mashahi-
di wa mambo hayo,[n] na pia roho
takatifu,[o] ambayo Mungu ame-
wapa wale wanaomtii yeye aki-
wa mtawala."

33 Waliposikia hayo, wakahi-
si wamechomwa sana nao waka-
taka kuwaangamiza.[p] **34** La-
kini mtu fulani akasimama kati-
ka Sanhedrini, Farisayo anaye-
itwa Gamalieli,[q] mwalimu wa
Sheria mwenye kuheshimiwa na
watu wote, akaamuru watu
hao watolewe nje kwa muda ki-
dogo.[r] **35** Naye akawaambia:
"Wanaume wa Israeli,[s] jianga-
lieni ninyi wenyewe kuhusu ja-
mbo mnalokusudia kuwatendea

watu hawa. **36** Kwa mfano,
kabla ya siku hizi Theuda alisimama, akisema yeye mwenyewe alikuwa mtu wa maana,[a] na wanaume kadhaa, karibu mia nne, wakajiunga na chama chake.[b] Lakini aliangamizwa, na wote waliokuwa wakimtii wakatawanywa na kumalizwa.
37 Baada yake Yuda Mgalilaya akainuka katika zile siku za uandikishaji,[c] naye akavuta watu wamfuate. Na bado mtu huyo aliangamia, na wale wote waliokuwa wakimtii wakatapanywa kotekote. **38** Na kwa hiyo, chini ya hali zilizopo, ninawaambia ninyi, Msijiingize katika mambo ya watu hawa, bali waacheni; (kwa sababu, ikiwa mpango huu au kazi hii imetoka kwa wanadamu, itaangamizwa;[d] **39** lakini ikiwa imetoka kwa Mungu,[e] hamtaweza kuwaangamiza;)[f] ama sivyo, huenda mkaonwa kuwa kwa kweli mnapigana na Mungu."[g] **40** Ndipo wakamsikiliza, nao wakawaita mitume, wakawapiga viboko,[h] na kuwaagiza waache kusema juu ya msingi wa jina la Yesu,[i] kisha wakawaacha waende zao.

41 Kwa hiyo, wakatoka mbele ya Sanhedrini, wakishangilia[j] kwa sababu walikuwa wamehesabiwa kuwa wenye kustahili kuvunjiwa heshima kwa ajili ya jina lake.[k] **42** Na kila siku katika hekalu na nyumba kwa nyumba[l] wakaendelea bila kuacha kufundisha[m] na kutangaza habari njema juu ya Kristo, Yesu.[n]

6 Basi katika siku hizo, wanafunzi walipokuwa wakiongezeka, Wayahudi wenye kusema Kigiriki[o] walianza kunung'unika juu ya Wayahudi wenye kusema Kiebrania, kwa sababu wajane wao walikuwa hawaangaliwi katika ugawaji wa kila siku.[a] **2** Kwa hiyo wale kumi na wawili wakauita umati wa wanafunzi na kusema: "Si vyema sisi kuliacha neno la Mungu ili kugawa chakula mezani.[b] **3** Kwa hiyo, akina ndugu, jitafutieni[c] wanaume saba waliothibitishwa kutoka kati yenu, wenye kujaa roho na hekima,[d] ili tupate kuwaweka rasmi juu ya kazi hii ya lazima; **4** lakini sisi tutajitoa kwa sala na kwa huduma ya neno."[e] **5** Na jambo hilo lililosemwa likaupendeza umati wote, nao wakamchagua Stefano, mwanamume mwenye kujaa imani na roho takatifu,[f] na Filipo[g] na Prokoro na Nikanori na Timoni na Parmena na Nikolao, mgeuzwa-imani wa Antiokia; **6** nao wakawaweka mbele ya mitume, na, wakiisha kusali, hao wakaweka mikono[h] yao juu yao.

7 Kwa sababu hiyo neno la Mungu likaendelea kukua,[i] na hesabu ya wanafunzi ikazidi kuongezeka sana katika Yerusalemu;[j] na umati mkubwa wa makuhani[k] ukaanza kuitii[l] imani.

8 Sasa Stefano, akiwa amejaa neema na nguvu, alikuwa akifanya mambo makubwa ya ajabu na ishara[m] kati ya watu.
9 Lakini watu fulani wakasimama kati ya wale waliokuwa wakitoka katika lile lililoitwa Sinagogi la Watu Waliowekwa Huru, na kati ya Wakirene na Waaleksandria[n] na kati ya wale wa kutoka Kilikia[o] na Asia, ili kubishana na Stefa-

SURA 5
a Mdo 8:9
b Mdo 21:38
c Lu 2:2
d Zb 127:1
Met 21:30
Mt 15:13
e Isa 26:12
Ro 8:31
f Isa 8:10
g Mdo 26:14
h Mt 10:17
Mk 13:9
Lu 20:10
Mdo 22:19
i Mdo 4:18
j Mt 5:12
Mdo 16:25
Ro 5:3
2Ko 12:10
Flp 1:29
Ebr 10:34
1Pe 4:13
k Mdo 9:16
l Mdo 20:20
m Mdo 2:46
Mdo 4:31
Mdo 18:5
n 2Ko 10:14

SURA 6
o Mdo 9:29

Safu ya 2
a Mdo 4:35
1Ti 5:3
Yak 1:27
b Kut 18:18
c Kum 1:13
d Mdo 6:10
Mdo 16:2
1Ti 3:7
e Mdo 2:42
f Mdo 11:24
g Mdo 21:8
h Kum 34:9
Mdo 8:17
Mdo 13:3
Mdo 14:23
1Ti 4:14
1Ti 5:22
2Ti 1:6
i Mdo 12:24
Mdo 19:20
j Mdo 2:47
k Yoh 12:42
Mdo 15:5
l Ro 16:26
m Mdo 2:43
n Mdo 18:24
o Mdo 23:34

no; **10** na bado hawakuweza
kufaulu katika pambano juu
ya hekima[a] na roho aliyoku-
wa akisema kwayo.[b] **11** Ndi-
po kwa siri wakashawishi watu
kusema:[c] "Tumemsikia akise-
ma maneno ya makufuru[d] juu
ya Musa na Mungu." **12** Nao
wakawachochea watu na wana-
ume wazee na waandishi, wa-
kamjia ghafula, wakamchu-
kua kwa nguvu na kumpele-
ka mpaka kwenye Sanhedrini.[e]
13 Nao wakatokeza mashahidi
wa uwongo,[f] waliosema: "Mtu
huyu haachi kusema mambo
yasiyofaa juu ya mahali hapa
patakatifu na juu ya Sheria.[g]
14 Kwa mfano, tumemsikia
akisema kwamba huyu Yesu
Mnazareti atapaangusha chini
mahali hapa na kuzibadili de-
sturi ambazo Musa alitukabi-
dhi."

15 Na wote waliokuwa wa-
meketi katika Sanhedrini wa-
lipokuwa wakimkazia macho,[h]
wakaona kwamba uso wake uli-
kuwa kama uso wa malaika.[i]

7 Lakini kuhani mkuu aka-
sema: "Je, mambo haya
ndivyo yalivyo?" **2** Akasema:
"Wanaume, akina ndugu na
akina baba, sikieni. Mungu wa
utukufu[j] alimtokea babu yetu
Abrahamu alipokuwa Meso-
potamia, kabla ya kuanza ku-
kaa Harani,[k] **3** naye aka-
mwambia, 'Toka katika nchi
yako na kutoka kwa watu wa
jamaa yako na uje mpaka ka-
tika nchi ambayo nitakuonye-
sha.'[l] **4** Ndipo akatoka nchi
ya Wakaldayo na kuanza kukaa
Harani. Na kutoka huko, baa-
da ya baba yake kufa,[m] Mungu
akamfanya abadili makao yake

SURA 6

a Lu 21:15
Mdo 6:3
b Isa 54:17
Lu 21:15
c Kut 23:1
Law 19:16
d 1Fa 21:10
Mt 26:59
e Lu 22:66
f Kum 5:20
Met 19:28
g Yer 26:11
Mdo 21:28
h Mt 10:17
i Amu 13:6

SURA 7

j Zb 29:3
k Mwa 11:31
Mwa 15:7
Ne 9:7
l Mwa 12:1
m Mwa 11:32
Ebr 11:8

Safu ya 2

a Mwa 12:4
b Kum 2:5
c Mwa 17:8
Kut 6:8
d Mwa 48:4
Kum 32:49
Ne 9:24
e Mwa 12:7
Mwa 13:15
f Mwa 15:13
Zb 39:12
1Pe 2:11
g Kut 12:40
h Mwa 15:13
i Mwa 15:14
j Kut 3:12
k Mwa 17:10
l Mwa 21:1
m Mwa 21:4
Law 12:3
Lu 2:21
n Mwa 29:32
o Mwa 37:11
p Mwa 37:28
Mwa 45:4
Zb 105:17
q Mwa 39:2
r Mwa 41:40
Mwa 41:41
Mwa 41:46
Zb 105:21
s Mwa 41:54
Mwa 42:5
t Mwa 42:2
u Mwa 42:6
v Mwa 45:1
w Mwa 45:16

mpaka kwenye nchi hii amba-
mo ninyi sasa mnakaa.[a] **5** Na
bado hakumpa urithi wowote
ndani yake, hapana, hata upa-
na wa wayo mmoja wa mguu;[b]
bali aliahidi kumpa hiyo kuwa
miliki,[c] na uzao wake baada
yake,[d] alipokuwa bado hana
mtoto.[e] **6** Zaidi ya hayo, Mu-
ngu alisema hivi, kwamba uzao
wake ungekuwa wakaaji wage-
ni[f] katika nchi ya kigeni[g] na
watu hao wangewafanya watu-
mwa na kuwatesa kwa miaka
mia nne.[h] **7** 'Na taifa ambalo
watalitumikia nitalihukumu,'[i]
Mungu akasema, 'na baada ya
mambo hayo watatoka na ku-
nitolea utumishi mtakatifu ma-
hali hapa.'[j]

8 "Alimpa pia agano la to-
hara;[k] na kwa hiyo aka-
mzaa Isaka[l] na kumtahiri siku
ya nane,[m] na Isaka akamzaa
Yakobo, na Yakobo akawazaa
wale vichwa vya familia kumi
na wawili.[n] **9** Na wale vichwa
vya familia wakamwonea Yo-
sefu wivu[o] na kumuuza Misri.[p]
Lakini Mungu alikuwa pamoja
naye,[q] **10** naye akamkomboa
kutoka katika dhiki zake zote
na kumpa neema na hekima
machoni pa Farao mfalme wa
Misri. Naye akamweka aongo-
ze Misri na nyumba yake yote.[r]
11 Lakini njaa ikaja juu ya Mi-
sri yote na Kanaani, hata dhiki
kuu; na mababu zetu hawaku-
wa wakipata chakula chocho-
te.[s] **12** Lakini Yakobo akasi-
kia kulikuwa na vyakula Mi-
sri[t] naye akawatuma mababu
zetu mara ya kwanza.[u] **13** Na
mara ya pili Yosefu akajuli-
shwa kwa ndugu zake;[v] na
ukoo wa familia ya Yosefu uka-
julishwa kwa Farao.[w] **14** Kwa

hiyo Yosefu akatuma watu wa-
mwite Yakobo baba yake na ja-
maa zake wote kutoka hapo,[a]
wenye kufikia hesabu ya nafsi
75.[b] **15** Yakobo akashuka kui-
ngia Misri.[c] Naye akafa;[d] na pia
mababu zetu,[e] **16** nao waka-
hamishwa mpaka Shekemu[f] na
kulazwa katika kaburi[g] ambalo
Abrahamu alikuwa amenunua
kwa bei fulani kwa fedha ku-
toka kwa wana wa Hamori ka-
tika Shekemu.[h]

17 "Wakati ulipokuwa ukika-
ribia kwa ajili ya utimizo wa aha-
di ambayo Mungu alikuwa ame-
mtangazia Abrahamu waziwa-
zi, watu wakaongezeka na
kuzidi katika Misri,[i] **18** mpa-
ka akainuka mfalme tofauti juu
ya Misri, ambaye hakujua haba-
ri za Yosefu.[j] **19** Huyo akatu-
mia hila ya serikali juu ya ja-
mii[k] yetu na kulazimisha ki-
makosa akina baba wawatupe
watoto wao wachanga, ili wasi-
hifadhiwe hai.[l] **20** Katika wa-
kati huo maalumu Musa aka-
zaliwa,[m] naye alikuwa mwenye
sura nzuri[n] machoni pa Mu-
ngu. Naye akanyonyeshwa kwa
miezi mitatu nyumbani mwa
baba yake. **21** Lakini alipotu-
pwa, binti ya Farao akamwo-
kota na kumlea kama mwana
wake mwenyewe.[o] **22** Kwa
sababu hiyo Musa akafundi-
shwa hekima[p] yote ya Wamisri.
Kwa kweli, yeye alikuwa mwe-
nye nguvu katika maneno[q] na
matendo.

23 "Sasa wakati wa mwa-
ka wake wa 40 ulipokuwa uki-
timia, wazo likaingia moyoni
mwake, awakague ndugu zake,
wana wa Israeli.[r] **24** Naye ali-
pomwona mtu fulani akitende-
wa isivyo haki, akamtetea na

SURA 7

a Mwa 45:9
b Mwa 46:27
Kum 10:22
c Mwa 46:29
Kum 26:5
d Mwa 49:33
e Kut 1:6
f Mwa 50:13
g Kut 13:19
Yos 24:32
h Mwa 23:16
i Kut 1:7
j Kut 1:8
k Kut 1:10
l Kut 1:22
m Kut 2:2
n Ebr 11:23
o Kut 2:5
Kut 2:10
p 1Fa 4:30
q Kut 11:3
Lu 24:19
r Kut 2:11

Safu ya 2

a Kut 2:12
b Ebr 11:26
c Mwa 13:8
d Kut 2:13
e Mdo 7:35
f Kut 2:14
g Kut 2:15
h Kut 2:22
Kut 18:3
i Kut 3:2
Isa 63:9
j Kut 3:3
k Mwa 50:24
Kut 3:6
Mk 12:26
Lu 20:37
l Kut 3:5
Yos 5:15
m Kut 3:7
Kum 26:7
n Kut 2:24

kulipiza kisasi kwa ajili ya yule
mwenye kutendewa vibaya kwa
kumpiga na kumuua Mmisri.[a]
25 Alikuwa akidhani ndugu
zake wangefahamu ya kwa-
mba Mungu alikuwa akiwapa
wokovu kwa mkono wake,[b]
lakini hawakufahamu hilo.
26 Na siku iliyofuata akawa-
tokea walipokuwa wakipigana,
naye akajaribu kuwapatanisha
tena wawe na amani,[c] akise-
ma, 'Wanaume, ninyi ni ndugu.
Kwa nini mnatendeana isivyo
haki?'[d] **27** Lakini yule aliye-
kuwa akimtendea jirani yake
isivyo haki akamsukuma mba-
li, akisema, 'Ni nani aliyekuwe-
ka wewe kuwa mtawala na
mwamuzi juu yetu?[e] **28** Una-
taka kuniangamiza vile ulivyo-
mwangamiza yule Mmisri jana,
sivyo?'[f] **29** Kwa maneno hayo
Musa akakimbia na kuwa mka-
aji mgeni katika nchi ya Mi-
diani,[g] ambako alizaa wana
wawili.[h]

30 "Na miaka 40 ilipotimia,
malaika akamtokea katika
mwali wa moto wa mti wa mi-
iba katika nyika ya Mlima Si-
nai.[i] **31** Sasa Musa alipouona
akastaajabia maono hayo.[j] La-
kini alipokuwa akikaribia ili
kuchunguza, sauti ya Yehova
ikaja, **32** 'Mimi ni Mungu wa
mababu zako, Mungu wa Abra-
hamu na wa Isaka na wa Yako-
bo.'[k] Akitetemeka, Musa ha-
kuthubutu kuchunguza zaidi.
33 Yehova akamwambia, 'Vua
viatu kutoka miguuni, kwa
maana mahali ambapo umesi-
mama ni udongo mtakatifu.[l]
34 Kwa hakika nimeona jinsi
watu wangu walio Misri[m] wa-
navyotendewa vibaya, nami ni-
mesikia kuugua[n] kwao na ni-

meshuka ili kuwakomboa.[a] Na
sasa njoo, nitakutuma uende
Misri.'[b] **35** Musa huyo, amba-
ye hao walimkana, wakisema,
'Ni nani aliyekuweka wewe
kuwa mtawala na mwamuzi?'[c]
mtu huyo Mungu alimtuma[d] ae-
nde akiwa mtawala na pia mko-
mbozi kwa mkono wa malaika
aliyemtokea katika mti wa mii-
ba. **36** Mtu huyo aliwaongoza
watoke[e] baada ya kufanya ma-
mbo ya ajabu na ishara katika
Misri[f] na katika Bahari Nyeku-
ndu[g] na katika nyika kwa mia-
ka 40.[h]
37 "Huyo ndiye Musa aliye-
waambia wana wa Israeli, 'Mu-
ngu atawainulia kutoka kati ya
ndugu zenu nabii kama mimi.'[i]
38 Huyo ndiye[j] aliyekuja kuwa
katikati ya kutaniko[k] katika
nyika pamoja na malaika[l] ali-
yesema naye juu ya Mlima Si-
nai na pamoja na mababu zetu,
naye akapokea maneno mata-
katifu[m] yaliyo hai ili awape
ninyi. **39** Mababu zetu wali-
kataa kumtii, bali wakamsu-
kuma kando[n] na katika mioyo
yao wakageuka kurudi Misri,[o]
40 wakimwambia Haruni, 'Tu-
fanyie miungu iende mbele
yetu. Kwa maana huyo Musa,
aliyetuongoza kutoka katika
nchi ya Misri, hatujui lililo-
mpata.'[p] **41** Kwa hiyo waka-
fanya ndama siku hizo[q] wa-
kaileteа hiyo sanamu dhabi-
hu na kuanza kujifurahisha
katika kazi za mikono yao.[r]
42 Kwa hiyo Mungu akageu-
ka na kuwakabidhi[s] watoe utu-
mishi mtakatifu kwa jeshi la
mbinguni, kama vile ambavyo
imeandikwa katika kitabu cha
manabii,[t] 'Je, mimi ndiye mli-
yetolea wanyama na dhabihu
nyikani kwa miaka 40, Ee nyu-
mba ya Israeli?[a] **43** Bali mli-
chukua hema la Moloki[b] na nyo-
ta[c] ya mungu Refani, maumbo
mliyoyafanya ili kuyaabudu.
Kwa sababu hiyo nitawahami-
shia[d] ninyi ng'ambo ya Babi-
loni.'
44 "Mababu zetu walikuwa
na hema la ushahidi nyikani,
kama vile alivyotoa maagizo ali-
pokuwa akisema na Musa ili ku-
lifanya kulingana na mfano ali-
okuwa ameuona.[e] **45** Na ma-
babu zetu waliolirithi waliliin-
giza pamoja na Yoshua[f] ndani
ya nchi iliyomilikiwa na mataifa,[g]
ambayo Mungu aliyafukuza
kutoka mbele ya mababu zetu.[h]
Lilibaki humo mpaka siku za
Daudi. **46** Alipata kibali[i] ma-
choni pa Mungu na kuomba
pendeleo la kuandaa makao[j]
kwa ajili ya Mungu wa Yakobo.
47 Hata hivyo, Sulemani ali-
mjengea nyumba.[k] **48** Inga-
wa hivyo, Aliye Juu Zaidi hakai
katika nyumba zilizofanywa
kwa mikono;[l] kama vile nabii
anavyosema, **49** 'Mbingu ni
kiti changu cha ufalme,[m] nayo
dunia ni kiti cha miguu[n] yangu.
Mtanijengea nyumba ya aina
gani? Asema Yehova. Au maha-
li pangu pa kupumzika pako
wapi?[o] **50** Mikono yangu ilifa-
nya vitu vyote hivi, sivyo?'[p]
51 "Ninyi watu wenye shi-
ngo ngumu na wasiotahiriwa
katika mioyo[q] na masikio, si-
kuzote mnaipinga roho taka-
tifu; kama mababu zenu wa-
livyofanya, ndivyo ninyi mna-
vyofanya.[r] **52** Ni yupi kati
ya manabii ambaye maba-
bu zenu hawakumtesa?[s] Ndi-
yo, waliwaua[t] wale waliotanga-
za kimbele kuhusu kuja kwa

SURA 7

a Kut 3:8
b Kut 3:10
c Kut 2:14
Mdo 7:27
d Kut 4:19
e Kut 12:41
f Kut 7:3
Kut 8:5
Kut 9:10
Zb 105:27
g Kut 14:21
Kut 15:5
Ebr 11:29
h Kut 16:35
Hes 14:33
i Kum 18:15
Mdo 3:22
j Kut 19:3
k Kum 5:27
l Kum 5:4
Isa 63:9
Mdo 7:53
Ga 3:19
Ebr 2:2
m Kut 21:1
Kum 9:10
Ro 3:2
1Pe 4:11
n Hes 14:3
o Kut 16:3
p Kut 32:1
Kut 32:23
q Kut 32:4
Kum 9:16
r Kut 32:6
Zb 106:19
s Zb 81:12
Ro 1:24
2Th 2:11
t 2Fa 17:16
Yer 7:18

Safu ya 2

a Amo 5:25
b 1Fa 11:7
c Kum 4:19
Amo 5:26
d Yer 25:11
Yer 29:10
Amo 5:27
e Kut 25:40
Ebr 8:5
f Kum 3:28
Kum 31:3
Yos 3:14
g Mwa 17:8
Ne 9:24
h Yos 23:9
Yos 24:18
i Zb 89:20
j 2Sa 7:2
1Nya 22:7
Zb 132:5
k 1Fa 6:1
1Nya 17:12
2Nya 3:1
l Isa 66:1
Mdo 17:24
m Zb 11:4
Mt 5:34
n Mt 5:35
o Isa 66:1
p Ebr 3:4
q Law 26:41
Kum 10:16
r Isa 1:4
Isa 63:10
Yer 6:10
s 2Nya 36:16
t Mt 23:31

Aliye mwadilifu,[a] ambaye ninyi sasa mmemsaliti na kumuua,[b] **53** ninyi mliopokea Sheria kama ilivyopitishwa na malaika[c] lakini hamkuishika."

54 Basi, waliposikia mambo hayo wakahisi wamechomwa mioyoni[d] mwao na kuanza kumsagia[e] meno yao. **55** Lakini yeye, akiwa amejaa roho takatifu, akakaza macho mbinguni, akaona utukufu wa Mungu na wa Yesu akiwa amesimama kwenye mkono wa kuume[f] wa Mungu, **56** naye akasema: "Tazameni! Ninaziona mbingu zimefunguka[g] na Mwana wa binadamu[h] akiwa amesimama kwenye mkono wa kuume[i] wa Mungu." **57** Ndipo wakapaaza sauti ya juu na kuweka mikono yao juu ya masikio yao,[j] wakamrukia wote pamoja. **58** Na baada ya kumtupa nje ya jiji,[k] wakaanza kumtupia mawe.[l] Na wale mashahidi[m] wakaweka chini mavazi yao ya nje miguuni pa kijana aliyeitwa Sauli.[n] **59** Nao wakaendelea kumtupia Stefano mawe huku akiomba na kusema: "Bwana Yesu, pokea roho yangu."[o] **60** Ndipo akapiga magoti yake, akapaaza sauti kubwa: "Yehova, usiwahesabie dhambi hii."[p] Na baada ya kusema hayo akalala usingizi katika kifo.

8 Naye Sauli alikuwa akikubaliana na kuuawa kwake.[q]

Katika siku hiyo mateso[r] makubwa yakatokea juu ya kutaniko lililokuwa katika Yerusalemu; wote isipokuwa mitume walitawanywa[s] kotekote katika maeneo ya Yudea na Samaria. **2** Lakini wanaume wenye kumheshimu Mungu wakamchukua Stefano kwenda kumzika,[a] nao wakafanya maombolezo[b] makubwa juu yake. **3** Ingawa hivyo, Sauli akaanza kushughulikia kutaniko kwa njia mbaya kabisa. Akawa akivamia nyumba moja baada ya nyingine, akiwakokota nje wanaume na wanawake, na kuwatia gerezani.[c]

4 Hata hivyo, wale waliokuwa wametawanywa wakapita katika nchi wakitangaza habari njema ya lile neno.[d] **5** Filipo akashuka kwenda jiji la Samaria[e] na kuanza kuwahubiria juu ya Kristo. **6** Kwa umoja umati ulikuwa ukisikiliza kwa makini mambo ambayo Filipo alikuwa akisema huku ukisikiliza na kutazama ishara alizokuwa akifanya. **7** Kwa maana wengi walikuwa na roho wachafu,[f] na roho hao walikuwa wakipaaza sauti kubwa na kutoka. Zaidi ya hayo, wengi waliokuwa wamepooza[g] na walio vilema waliponywa. **8** Kwa hiyo kukawa na shangwe kubwa katika jiji hilo.[h]

9 Sasa katika jiji hilo kulikuwa na mtu fulani aliyeitwa Simoni, ambaye, kabla ya hili, alikuwa akifanya ufundi wa uchawi[i] na kushangaza taifa la Samaria, akisema yeye mwenyewe alikuwa mtu mkuu.[j] **10** Na wote, mdogo kwa mkubwa, walikuwa wakimkazia uangalifu na kusema: "Mtu huyu ndiye Nguvu za Mungu, zinazoweza kuitwa Kuu." **11** Kwa hiyo walikuwa wakimsikiliza kwa sababu alikuwa amewashangaza kwa muda fulani kwa ufundi wake wa uchawi. **12** Lakini walipomwamini Filipo, aliyekuwa akitangaza haba-

SURA 7
a Mdo 3:14
1Yo 2:1
b Isa 53:8
c Mdo 7:38
Ga 3:19
Ebr 2:2
d Mdo 5:33
e Zb 35:16
Zb 112:10
f Zb 110:1
Mt 26:64
g Eze 1:1
Mt 3:16
Yoh 1:51
h Da 7:13
i Ro 8:34
Efe 1:20
Kol 3:1
j Zek 7:11
Lu 16:24
k 1Fa 21:13
Ebr 13:12
l Law 24:16
Mt 23:37
m Kum 17:7
Yoh 16:2
n Mdo 8:1
Mdo 22:20
o Zb 31:5
p Mt 5:44

SURA 8
q Mdo 7:58
r Mdo 11:19
s Mt 10:23

Safu ya 2
a Mt 14:12
b Mwa 50:10
c Mdo 9:1
Mdo 22:4
Mdo 26:10
1Ko 15:9
Ga 1:13
Flp 3:6
d Isa 52:7
Mdo 11:19
e Mdo 1:8
f Mt 10:1
Mk 6:7
g Mdo 9:33
h Yoh 4:42
i Mdo 13:6
j Mdo 5:36

ri njema ya ufalme wa Mungu[a]
na juu ya jina la Yesu Kristo,
wakabatizwa, wanaume na pia
wanawake.[b] **13** Simoni mwe-
nyewe pia akawa mwamini, na,
baada ya kubatizwa, akawa aki-
mhudumia Filipo[c] daima; naye
alishangaa kuona ishara na
kazi kubwa zenye nguvu zikite-
ndeka.

14 Wakati mitume katika Ye-
rusalemu waliposikia kwamba
Samaria ilikuwa imelikubali
neno la Mungu,[d] wakawatuma
Petro na Yohana kwao; **15** na
hawa wakashuka kwenda na
kusali kwa ajili yao wapate
roho takatifu.[e] **16** Kwa maa-
na ilikuwa bado haijamwangu-
kia yeyote kati yao, bali wa-
likuwa wamebatizwa tu katika
jina la Bwana Yesu.[f] **17** Ndipo
wakaanza kuweka mikono yao
juu yao,[g] nao wakaanza kupo-
kea roho takatifu.

18 Sasa Simoni alipoona
kwamba roho ilitolewa kupitia
kuwekewa mikono ya mitume,
aliwatolea pesa,[h] **19** akisema:
"Nipeni mimi pia mamlaka hii,
ili yeyote ambaye nitaweka mi-
kono yangu juu yake apate ku-
pokea roho takatifu." **20** La-
kini Petro akamwambia: "Fe-
dha yako na iangamie pamoja
nawe, kwa sababu ulitaka ku-
pata zawadi ya bure ya Mungu
kwa kutumia pesa.[i] **21** Wewe
huna sehemu wala fungu ka-
tika jambo hili, kwa maana
moyo wako si mnyoofu macho-
ni pa Mungu.[j] **22** Kwa hiyo,
tubu ubaya wako huu, na umwo-
mbe Yehova dua[k] ili, ikiwezeka-
na, upate kusamehewa hila ya
moyo wako; **23** kwa maana
ninaona wewe ni nyongo yenye
sumu[l] na kifungo cha ukosefu

SURA 8

a Lu 8:1

b Mt 28:19
Mdo 18:8

c Mdo 6:5

d Mdo 11:1

e Mt 16:19

f Mdo 10:48
Mdo 19:2

g Mdo 6:6
Mdo 19:6
2Ti 1:6

h Mik 3:11
1Ti 6:5

i Mt 10:8
Mdo 10:45

j Zb 78:37
Efe 5:5

k Isa 55:7
Da 4:27

l Kum 29:18

Safu ya 2

a Ebr 12:15

b Kut 8:8
Hes 21:7
1Fa 13:6
Yak 5:16

c Mt 9:35
Mdo 1:8

d Zb 34:7
Ebr 1:14
Ufu 14:6

e Isa 56:4

f Yer 13:23
Sef 3:10

g 2Nya 6:32
Yoh 12:20

h Mdo 17:11

i Mdo 10:19

wa uadilifu."[a] **24** Simoni aka-
jibu akasema: "Ninyi, mwombe-
ni Yehova dua[b] kwa ajili yangu
ili hata moja kati ya mambo mli-
yosema lisinipate."

25 Kwa hiyo, walipokuwa
wametoa ushahidi kikamili na
wakiwa wamelisema neno la
Yehova, wakarudi Yerusalemu,
nao wakaenda wakitangaza ha-
bari njema kwenye vijiji vingi
vya Wasamaria.[c]

26 Hata hivyo, malaika[d] wa
Yehova akasema na Filipo,
akamwambia: "Ondoka uende
upande wa kusini kwenye bara-
bara inayoshuka kutoka Yeru-
salemu mpaka Gaza." (Hii ni ba-
rabara ya jangwani.) **27** Ndi-
po akaondoka akaenda, na, ta-
zama! towashi[e] Mwethiopia,[f]
mwanamume aliye na mamlaka
chini ya Kandake malkia wa
Waethiopia, na ambaye aliku-
wa juu ya hazina yote ya ma-
lkia. Huyo alikuwa ameenda
Yerusalemu kuabudu,[g] **28** la-
kini alikuwa anarudi naye ali-
kuwa ameketi katika gari lake,
akimsoma kwa sauti kubwa na-
bii Isaya.[h] **29** Kwa hiyo roho
ikamwambia[i] Filipo: "Karibia
ujiunge na gari hili." **30** Fi-
lipo akakimbia kandokando na
kumsikia akimsoma kwa sauti
kubwa nabii Isaya, naye akase-
ma: "Je, wewe kwa kweli unae-
lewa unayoyasoma?" **31** Aka-
sema: "Kwa kweli, ninawezaje
kuelewa, mtu fulani asiponio-
ngoza?" Naye akamsihi Fili-
po apande na kuketi pamo-
ja naye. **32** Sasa kifungu cha
Andiko alichokuwa akisoma
kwa sauti kubwa kilikuwa hiki:
"Kama kondoo aliletwa ma-
chinjioni, na kama mwana-ko-
ndoo asiye na sauti mbele ya

mwenye kumnyoa, ndivyo huyo
asivyofungua kinywa chake.[a]
33 Wakati wa kufedheheshwa
kwake hukumu iliondolewa
mbali naye.[b] Ni nani atakayeele-
za kirefu habari za kizazi cha-
ke? Kwa sababu uhai wake una-
ondolewa kutoka duniani."[c]

34 Yule towashi akamjibu
akamwambia Filipo: "Ninakuo-
mba, Nabii anasema hivyo juu
ya nani? Juu yake mwenye-
we au juu ya mtu mwingine?"
35 Filipo akafungua kinywa
chake,[d] akaanza na Andiko[e]
hilo, akamtangazia habari nje-
ma juu ya Yesu. **36** Sasa wa-
lipokuwa wakienda juu ya ile
barabara, wakafika mahali pe-
nye maji, na towashi akasema:
"Tazama! Maji; ni nini kinacho-
nizuia nisibatizwe?"[f] **37** ——
38 Ndipo akaamuru gari lisi-
mame, nao wote wawili waka-
shuka na kuingia ndani ya maji,
Filipo na pia towashi; naye aka-
mbatiza. **39** Walipokuwa wa-
mepanda kutoka ndani ya maji,
roho ya Yehova ikamwondoa Fi-
lipo upesi,[g] na towashi haku-
mwona tena kamwe, kwa ma-
ana aliendelea kwenda zake
akishangilia. **40** Lakini Fili-
po akaonekana Ashdodi, naye
akaenda akipita katika eneo
hilo na kuendelea kuyatanga-
zia[h] majiji yote habari njema
mpaka alipofika Kaisaria.[i]

9 Lakini Sauli, bado akiwati-
sha wanafunzi[j] wa Bwana
na akitaka kuwaua,[k] akamwe-
ndea kuhani mkuu **2** na ku-
mwomba barua za kwenda
kwenye masinagogi katika Da-
masko, ili apate kuwaleta Yeru-
salemu wakiwa wamefungwa
wowote ambao angewapata wa-

SURA 8
a Isa 53:7
1Pe 2:23
b Mt 26:59
c Isa 53:8
Da 9:26
Flp 2:8
d Mt 13:52
e Mdo 18:28
2Ti 3:16
f Mdo 10:47
g 1Fa 18:12
h Lu 9:6
i Mdo 21:8

SURA 9
j Mdo 8:3
Ga 1:13
1Ti 1:13
k Mdo 22:4
Mdo 26:11

Safu ya 2
a Mdo 9:14
Mdo 11:26
Mdo 22:4
Mdo 24:14
b Mdo 22:6
c 1Ko 15:8
d Mt 25:40
e Mdo 9:11
f Mdo 22:9
Mdo 26:13
g Da 10:7
h Mdo 22:9
i Mdo 22:11
j Mdo 13:11
k Mdo 22:12
l Mdo 11:25
Mdo 21:39
Mdo 22:3
m Mdo 9:17

lio wa Ile Njia,[a] wanaume na wa-
nawake.

3 Basi alipokuwa akisafiri,
akakaribia Damasko, na ghafu-
la nuru kutoka mbinguni ika-
mulika kumzunguka,[b] **4** naye
akaanguka chini na kusikia sa-
uti ikimwambia: "Sauli, Sauli,
kwa nini unanitesa?"[c] **5** Aka-
sema: "Wewe ni nani, Bwana?"
Akasema: "Mimi ni Yesu, amba-
ye wewe unatesa.[d] **6** Hata hi-
yo, simama[e] uingie jijini, nawe
utaambiwa jambo unalopaswa
kufanya." **7** Basi wanaume
waliokuwa wakisafiri pamo-
ja naye[f] walikuwa wamesima-
ma wakiwa hawana la kusema,[g]
wakisikia, kwa kweli, sauti,[h] la-
kini bila kumwona mtu yeyo-
te. **8** Lakini Sauli akainuka,
na ingawa macho yake yaliku-
wa yamefunguka hakuwa aki-
ona kitu.[i] Kwa hiyo wakamwo-
ngoza kwa kumshika mkono na
kumpeleka Damasko. **9** Na
kwa siku tatu hakuona kitu
chochote,[j] naye hakula wala ku-
nywa.

10 Katika Damasko kuliku-
wa na mwanafunzi fulani aliye-
itwa Anania,[k] naye Bwana aka-
mwambia katika maono: "Ana-
nia!" Akasema: "Mimi hapa,
Bwana." **11** Bwana akamwa-
mbia: "Ondoka, uende kwenye
barabara inayoitwa Nyoofu, na
kwenye nyumba ya Yuda tafuta
mtu anayeitwa jina Sauli, kuto-
ka Tarso.[l] Kwa maana, tazama!
anasali, **12** na katika maono
amemwona mwanamume ana-
yeitwa Anania akiingia na ku-
weka mikono yake juu yake ili
apate kuona tena."[m] **13** Laki-
ni Anania akajibu: "Bwana,
nimesikia kutoka kwa wengi
juu ya mtu huyu, mambo me-

ngi mabaya aliyowatendea
watakatifu wako katika Yeru-
salemu. **14** Naye hapa ana
mamlaka kutoka kwa wakuu
wa makuhani kuwatia vifungo-
ni wale wote wanaoliitia jina
lako."[a] **15** Lakini Bwana aka-
mwambia: "Ondoka uende, kwa
sababu mtu huyu ni chombo ki-
lichochaguliwa[b] kwangu ili ku-
peleka jina langu kwa mataifa[c]
na vilevile kwa wafalme[d] na
wana wa Israeli. **16** Kwa ma-
ana nitamwonyesha wazi ni ma-
mbo mangapi ambayo atatese-
ke kwa ajili ya jina langu."[e]

17 Kwa hiyo Anania akaen-
da zake na kuingia katika
ile nyumba, naye akaweka mi-
kono yake juu yake na kuse-
ma: "Sauli, ndugu, yule Bwa-
na, yule Yesu aliyekutokea ka-
tika barabara uliyoijia, ame-
nituma, ili upate kuona tena
na kujazwa roho takatifu."[f]
18 Na mara moja kitu kilicho-
onekana kama magamba kika-
anguka kutoka kwenye macho
yake, naye akapata kuona tena;
naye akasimama na kubatizwa,
19 naye akala chakula na ku-
pata nguvu.[g]

Kwa siku kadhaa akapata
kuwa pamoja na wanafunzi ka-
tika Damasko,[h] **20** naye aka-
anza mara moja kumhubiri
Yesu[i] katika masinagogi, kwa-
mba Huyu ndiye Mwana wa
Mungu. **21** Lakini wote wali-
omsikia wakashangaa nao wa-
kawa wakisema: "Je, huyu si
yule mtu aliyewaangamiza[j]
wale walio katika Yerusalemu
wanaoliitia jina hilo, na aliye-
kuwa amekuja hapa kwa ku-
sudi hilo hilo, ili apate kuwa-
peleka wakiwa wamefungwa
kwa wakuu wa makuhani?"[k]

SURA 9

a 1Ko 1:2
2Ti 2:22
b Mdo 13:2
Ro 1:1
1Ti 1:12
c Ro 1:5
Ga 2:7
1Ti 2:7
d Mdo 25:22
Mdo 26:1
Mdo 27:24
e Mdo 20:23
Mdo 21:11
2Ko 11:23
Kol 1:24
2Ti 1:12
f Mdo 13:52
Mdo 22:13
g Zb 104:15
h Mdo 26:20
i Ga 1:16
j Mdo 8:3
Ga 1:13
Ga 1:23
k Mdo 9:2

Safu ya 2

a Mdo 17:3
Mdo 18:28
b Mdo 20:3
Mdo 23:12
2Ko 11:23
c 2Ko 11:32
d Yos 2:15
1Sa 19:12
2Ko 11:33
e Ga 1:18
f Mdo 4:36
g 1Ko 9:1
h Mdo 9:4
Mdo 22:7
i Mdo 9:20
j Mdo 4:29
k 2Ko 11:26
l Mdo 11:25
Ga 1:21
m Mdo 8:1

22 Lakini Sauli akaendelea ku-
pata nguvu hata zaidi naye ali-
kuwa akiwafadhaisha Waya-
hudi waliokuwa wakikaa Da-
masko alipokuwa akithibiti-
sha kupatana na akili kwamba
huyu ndiye Kristo.[a]

23 Sasa mwishoni mwa siku
nyingi, Wayahudi walikata sha-
uri pamoja kumwangamiza.[b]
24 Hata hivyo, hila yao juu
yake ikajulikana kwa Sauli. La-
kini walikuwa pia wakiyaangа-
lia sana malango mchana na
pia usiku ili kumwangamiza.[c]
25 Kwa hiyo wanafunzi wake
wakamchukua na kumshusha
usiku kupitia shimo ukutani,
wakamshusha katika kapu.[d]

26 Alipofika Yerusalemu[e]
akafanya jitihada za kujiunga
na wanafunzi; lakini wote wali-
kuwa wakimwogopa, kwa saba-
bu hawakuamini alikuwa mwa-
nafunzi. **27** Kwa hiyo Barna-
baa akaja kumsaidia[f] na ku-
mpeleka kwa mitume, naye
akawaambia kirefu jinsi alivyo-
kuwa amemwona Bwana[g] ka-
tika barabara, na kwamba ali-
kuwa amesema naye,[h] na jinsi
alivyokuwa amesema kwa uja-
siri katika jina la Yesu, kule
Damasko.[i] **28** Naye akakaa
pamoja nao, akitembea ndani
na nje katika Yerusalemu, aki-
sema kwa ujasiri katika jina la
Bwana;[j] **29** naye alikuwa aki-
ongea na kubishana na Waya-
hudi wenye kusema Kigiriki.
Lakini hao wakawa wakijaribu
kumwangamiza.[k] **30** Akina
ndugu walipogundua hilo, wa-
kamshusha mpaka Kaisaria na
kumtuma aende zake Tarso.[l]

31 Ndipo, kwa kweli, kutaniko[m]
kotekote katika Yudea na
Galilaya na Samaria likaingia

katika kipindi cha amani, likijengwa; nalo lilipokuwa likitembea katika kumwogopa Yehova[a] na katika faraja ya roho takatifu[b] likaendelea kuongezeka.

32 Sasa Petro alipokuwa akienda kupitia sehemu zote akashuka pia kwa watakatifu waliokuwa wakikaa Lida.[c] **33** Huko akapata mwanamume fulani aliyeitwa Ainea, ambaye alikuwa amelala juu ya kitanda chake kwa miaka minane, kwa kuwa alikuwa amepooza. **34** Naye Petro akamwambia:[d] "Ainea, Yesu Kristo anakuponya wewe.[e] Simama, utandike kitanda chako." Naye akasimama mara moja. **35** Na wale wote waliokuwa wakikaa Lida na katika nchi tambarare ya Sharoni[f] wakamwona, nao wakageuka kumwelekea Bwana.[g]

36 Lakini katika Yopa[h] kulikuwako mwanafunzi fulani aliyeitwa Tabitha, jina ambalo, linapotafsiriwa, linamaanisha Dorkasi. Huyo alizidi katika matendo mema[i] na zawadi za rehema alizokuwa akitoa. **37** Lakini ikawa kwamba katika siku hizo alishikwa na ugonjwa akafa. Kwa hiyo wakamwosha na kumlaza katika chumba cha juu. **38** Sasa kwa kuwa Lida palikuwa karibu na Yopa,[j] wanafunzi waliposikia kwamba Petro alikuwa katika jiji hilo wakatuma wanaume wawili kwake wakamsihi: "Tafadhali usikawie kuja kwetu." **39** Ndipo Petro akaondoka na kwenda pamoja nao. Naye alipofika, wakampeleka katika chumba cha juu; na wajane wote wakajitokeza kwake wakilia na kuonyesha mavazi mengi ya ndani na mavazi ya nje[a] ambayo Dorkasi alikuwa akitengeneza alipokuwa pamoja nao.[b] **40** Lakini Petro akamtoa kila mtu nje,[c] akapiga magoti, akasali, akageukia ule mwili, akasema: "Tabitha, inuka!" Akafungua macho yake na, alipomwona Petro, akaketi wima.[d] **41** Petro akampa mkono wake, akamwinua,[e] naye akawaita watakatifu na wajane na akamweka mbele yao akiwa hai.[f] **42** Jambo hilo likajulikana kotekote katika Yopa, na wengi wakamwamini Bwana.[g] **43** Petro akabaki Yopa[h] siku kadhaa pamoja na mtu fulani anayeitwa Simoni, mtengenezaji wa ngozi.[i]

10 Sasa katika Kaisaria kulikuwa na mwanamume fulani aliyeitwa jina Kornelio, ofisa-jeshi[j] wa kikosi[k] cha Italia, kama kilivyokuwa kikiitwa, **2** mtu mwenye kuheshimu[l] na kumwogopa[m] Mungu pamoja na watu wote wa nyumba yake, naye aliwapa watu[n] zawadi nyingi za rehema na kuomba dua kwa Mungu sikuzote.[o] **3** Karibu tu na saa tisa[p] ya mchana akaona wazi katika maono[q] malaika[r] wa Mungu akiingia kwake na kumwambia: "Kornelio!" **4** Mtu huyo akamtazama na, akiogopa, akasema: "Ni nini, Bwana?" Akamwambia: "Sala[s] na zawadi zako za rehema zimepanda kama ukumbusho mbele za Mungu.[t] **5** Kwa hiyo sasa tuma watu Yopa ukamwite Simoni anayeitwa Petro. **6** Mtu huyu ni mgeni wa Simoni, mtengenezaji wa ngozi, aliye na nyumba kando ya bahari."[u] **7** Mara tu

SURA 9
a Zb 86:11
b Yoh 14:16
c Mdo 9:38
d Mt 10:8
e Mdo 3:6
Mdo 4:10
f 1Nya 5:16
g Mdo 11:21
h 2Nya 2:16
i 1Ti 2:10
j Mdo 9:32

Safu ya 2
a Mt 5:40
b Isa 32:8
c Mk 5:40
Lu 8:51
d Mt 9:25
Lu 7:15
Yoh 11:43
e Mdo 3:7
f 1Fa 17:23
g Yoh 11:45
h Mk 6:10
i Mdo 10:6
Mdo 10:32

SURA 10
j Mt 8:5
k Mdo 27:1
l Mdo 8:2
Mdo 22:12
m Met 14:2
n Lu 7:5
Mdo 8:21
o Mt 7:7
p Mdo 3:1
q Mdo 9:10
r Lu 1:11
s Zb 65:2
Met 15:8
t Met 15:29
Da 10:12
Yoh 9:31
1Pe 3:12
u Mdo 9:43
Mdo 10:32

malaika aliyesema naye alipokuwa ameondoka, akawaita wawili kati ya watumishi wake wa nyumbani na askarijeshi mwenye kumwogopa Mungu kutoka kati ya wale waliokuwa wakimhudumia daima,[a] **8** naye akawasimulia kila kitu na kuwatuma kwenda Yopa.[b]

9 Siku iliyofuata walipokuwa wakiendelea na safari yao na wakikaribia jiji hilo, Petro akapanda juu ya paa[c] ya nyumba karibu saa sita ili kusali.[d] **10** Lakini akaona njaa sana naye akataka kula. Walipokuwa wakitayarisha, akapata njozi[e] **11** naye akaona mbingu imefunguliwa[f] na chombo cha namna fulani kikishuka kama shuka kubwa la kitani, kikishushwa juu ya dunia kwa ncha zake nne; **12** na ndani yake mlikuwa namna zote za viumbe wenye miguu minne na vitu vinavyotambaa vya dunia na ndege wa mbinguni.[g] **13** Na sauti ikamjia: "Simama, Petro, chinja ule!"[h] **14** Lakini Petro akasema: "Sivyo hata kidogo, Bwana, kwa sababu sijakula kamwe kitu chochote kilichotiwa unajisi na kisicho safi."[i] **15** Na sauti ikasema tena naye, mara ya pili: "Wewe acha kuviita najisi[j] vitu ambavyo Mungu ametakasa." **16** Jambo hilo likatokea mara ya tatu, na mara hiyo kile chombo kikachukuliwa juu mbinguni.[k]

17 Basi Petro alipokuwa amefadhaika sana ndani yake juu ya maana ya maono aliyokuwa ameona, tazama! wale watu waliotumwa na Kornelio walikuwa wameuliza kuhusu nyumba ya Simoni na walikuwa wamesimama hapo langoni.[a] **18** Nao wakapaaza sauti na kuuliza kama Simoni anayeitwa Petro alikuwa mgeni humo. **19** Petro alipokuwa akiwaza akilini mwake kuhusu yale maono, roho[b] ikasema: "Tazama! Wanaume watatu wanakutafuta. **20** Hata hivyo, simama, ushuke na kwenda pamoja nao, nawe usiwe na shaka hata kidogo, kwa sababu nimewatuma."[c] **21** Kwa hiyo Petro akashuka kutoka ghorofani mpaka kwa wanaume hao na kusema: "Tazameni! Mimi ndiye mnayetafuta. Kwa nini mko hapa?" **22** Wakasema: "Kornelio, ofisa-jeshi, mwanamume mwadilifu na mwenye kumwogopa Mungu[d] na mwenye sifa njema[e] katika taifa lote la Wayahudi, malaika mtakatifu alimpa maagizo ya Mungu kwamba atume watu ili uitwe uje nyumbani kwake apate kuyasikia mambo utakayosema." **23** Kwa hiyo akawakaribisha na kuwapa makao.

Siku iliyofuata akaondoka na kwenda pamoja nao, na baadhi ya akina ndugu waliokuwa wametoka Yopa wakaenda pamoja naye. **24** Siku ya pili yake akaingia Kaisaria. Bila shaka, Kornelio alikuwa akiwatarajia naye alikuwa amewaita pamoja jamaa zake na rafiki zake wa karibu sana. **25** Petro alipokuwa akiingia, Kornelio akakutana naye, akaanguka chini miguuni pake na kumsujudia. **26** Lakini Petro akamwinua, akisema: "Simama; mimi pia ni mwanadamu."[f] **27** Naye alipokuwa akiongea naye akaingia na kuwakuta watu wengi wakiwa

SURA 10

a Mt 8:9
b Mdo 11:13
c Kum 22:8
d Da 6:10
1Th 5:17
e Mdo 11:5
Mdo 22:17
f Eze 1:1
Mdo 7:56
Ufu 19:11
g Mdo 11:6
h Mdo 11:7
i Law 11:4
Law 11:13
Law 20:25
Kum 14:3
Kum 14:19
Eze 4:14
j Mt 15:11
Mdo 10:28
Ro 14:14
1Ti 4:4
Tit 1:15
k Mdo 11:10

Safu ya 2

a Mdo 11:11
b Mdo 13:2
Mdo 15:28
Mdo 16:6
Mdo 20:23
c Mdo 11:12
d Mdo 10:1
e Mdo 22:12
f Lu 4:8
Mdo 14:15
Ufu 19:10
Ufu 22:9

wamekusanyika, **28** naye
akawaambia: "Ninyi mnajua ji-
nsi ilivyo kinyume cha sheria
kwa Myahudi kujiunga na mtu
wa jamii nyingine au kumka-
ribia;[a] na bado Mungu ameni-
onyesha sipaswi kumwita mtu
yeyote kuwa najisi au si safi.[b]
29 Kwa sababu hiyo nikaja,
kwa kweli bila kupinga, nilipo-
itwa nije. Kwa hiyo ninawauli-
za ninyi ni sababu gani mliyo-
niitia."

30 Basi Kornelio akasema:
"Siku nne zilizopita kutoka
saa hii nilikuwa nikisali kati-
ka nyumba yangu saa tisa,[c]
wakati, tazama! mwanamume
aliyekuwa amevaa vazi linalo-
ng'aa[d] alisimama mbele yangu
31 na kusema, 'Kornelio, sala
yako imesikiwa na kukubaliw-
a, nazo zawadi zako za re-
hema zimekumbukwa mbele za
Mungu.[e] **32** Kwa hiyo, tuma
watu waende Yopa na kumwi-
ta Simoni, anayeitwa Petro.[f]
Mtu huyu ni mgeni katika nyu-
mba ya Simoni, mtengenezaji
wa ngozi, kando ya bahari.'[g]
33 Kwa hiyo mara moja nika-
tuma watu kwako, nawe uka-
fanya vema kuja hapa. Na kwa
hiyo wakati huu sisi sote tupo
mbele za Mungu kuyasikia ma-
mbo yote ambayo umeamriwa
na Yehova kusema."[h]

34 Ndipo Petro akafungua
kinywa chake na kusema: "Kwa
hakika ninaona kwamba Mu-
ngu hana ubaguzi,[i] **35** bali ka-
tika kila taifa mtu ambaye ana-
mwogopa na kutenda uadilifu
anakubalika kwake.[j] **36** Alitu-
ma[k] neno kwa wana wa Isra-
eli kuwatangazia habari nje-
ma ya amani[l] kupitia Yesu Kri-
sto: Huyu ni Bwana wa wengine
wote.[a] **37** Ninyi mnaijua ha-
bari iliyoongewa kotekote kati-
ka Yudea yote, kuanzia Galilaya
baada ya ubatizo aliohubiri Yo-
hana,[b] **38** yaani, Yesu aliye-
kuwa ametoka Nazareti, jinsi
Mungu alivyomtia mafuta kwa
roho takatifu[c] na nguvu, naye
akaenda akipita katika nchi
akitenda mema na kuwaponya
wote waliokandamizwa na Ibi-
lisi;[d] kwa sababu Mungu aliku-
wa pamoja naye.[e] **39** Nasi ni
mashahidi wa mambo yote ali-
yoyafanya katika nchi ya Wa-
yahudi na pia katika Yerusale-
mu; lakini walimwangamiza
pia kwa kumtundika mtini.[f]
40 Mungu alimfufua Huyu ka-
tika siku ya tatu na kumfu-
nua,[g] **41** si kwa watu wote,
bali kwa mashahidi waliowe-
kwa kimbele na Mungu,[h] kwe-
tu sisi, tuliokula na kunywa
pamoja naye[i] baada ya kufufu-
liwa kwake kutoka kwa wafu.
42 Pia, alituagiza sisi tuwahu-
birie[j] watu na kutoa ushahidi
kamili kwamba Huyu ndiye ali-
yeagizwa na Mungu kuwa mwa-
muzi wa walio hai na wafu.[k]
43 Kwake yeye manabii wote
hutoa ushahidi,[l] kwamba kila
mtu anayemwamini hupata
msamaha wa dhambi kupitia
jina lake."[m]

44 Petro alipokuwa bado
akisema juu ya mambo haya
roho takatifu ikawaangukia
wote waliokuwa wakisikia lile
neno.[n] **45** Na waaminifu wa-
liokuwa wamekuja pamoja na
Petro ambao walikuwa kati
ya wale waliotahiriwa waka-
shangaa, kwa sababu zawa-
di ya bure ya roho takatifu
ilikuwa ikimiminwa pia juu
ya watu wa mataifa.[o] **46** Kwa

SURA 10

a Yoh 4:9
Yoh 18:28
b Mdo 10:45
Mdo 15:8
Efe 3:6
c Mdo 11:13
d Mt 28:3
Mdo 1:10
e Da 10:12
Ebr 6:10
f Mdo 10:18
g Mdo 9:43
h Mdo 10:42
i Kum 10:17
2Nya 19:7
Ayu 34:19
Ro 2:11
Ga 2:6
j Ro 2:13
1Ko 12:13
Ga 3:28
k Zb 107:20
Zb 147:18
l Isa 52:7
Nah 1:15

Safu ya 2

a Da 7:14
Mt 28:18
Ro 14:9
Efe 1:20
Ufu 19:16
b Lu 4:14
c Isa 11:2
Isa 42:1
Isa 61:1
Mt 3:16
Ebr 1:9
d Lu 13:16
e Yoh 3:2
f Mdo 2:23
Ga 3:13
g Yon 1:17
Yon 2:10
Mdo 2:24
1Ko 15:4
h Yoh 14:22
i Lu 24:30
Yoh 21:13
j Mt 28:19
Mdo 1:8
k Yoh 5:22
Mdo 17:31
Ro 14:9
2Ko 5:10
2Ti 4:1
1Pe 4:5
l Isa 53:11
Yer 31:34
Eze 34:23
Da 9:24
Lu 24:27
Ufu 19:10
m Ro 10:11
Ga 3:22
n Mdo 4:31
Mdo 8:15
o Ga 3:14

maana waliwasikia wakisema
katika lugha na wakimtukuza
Mungu.[a] Ndipo Petro akajibu:
47 "Je, mtu yeyote anaweza
kuyakataza maji kwamba hawa
wasibatizwe[b] ambao wameipo-
kea roho takatifu kama vile
sisi tulivyoipokea?" **48** Ndi-
po akawaamuru wabatizwe ka-
tika jina la Yesu Kristo.[c] Ki-
sha wakamwomba akae pamo-
ja nao siku kadhaa.

11 Sasa mitume na ndugu
waliokuwa katika Yudea
wakasikia kwamba watu wa
mataifa[d] walikuwa pia wame-
pokea neno la Mungu. **2** Kwa
hiyo Petro alipopanda mpaka
Yerusalemu, waliokuwa wakiu-
nga mkono kutahiriwa[e] waka-
anza kushindana naye, **3** wa-
kisema aliingia ndani ya nyu-
mba ya watu ambao hawakuwa
wametahiriwa naye alikula pa-
moja nao. **4** Ndipo Petro aka-
waeleza waziwazi, akisema:

5 "Mimi nilikuwa katika jiji
la Yopa nikisali, na katika njo-
zi nikaona maono, chombo cha
namna fulani kikishuka kama
shuka kubwa la kitani, kiki-
shushwa kwa ncha zake nne
kutoka mbinguni, nacho kika-
ja moja kwa moja mahali nilipo-
kuwa. **6** Nilipotazama ndani
yake, nilichunguza na kuona
viumbe vya dunia vyenye mi-
guu minne na wanyama-mwi-
tu na vitu vinavyotambaa na
ndege wa mbinguni.[f] **7** Pia ni-
kasikia sauti ikiniambia, 'Si-
mama, Petro, chinja ule!'[g]
8 Lakini nikasema, 'Sivyo hata
kidogo, Bwana, kwa sababu
kitu najisi au kisicho safi haki-
japata kamwe kuingia ndani ya
kinywa changu.'[h] **9** Mara ya
pili sauti kutoka mbinguni ika-
jibu, 'Wewe acha kuviita najisi
vitu ambavyo Mungu ametaka-
sa.'[a] **10** Hilo likatokea mara
ya tatu, na kila kitu kikavutwa
juu tena kuingia mbinguni.[b]
11 Pia, tazama! wakati huohuo
wanaume watatu walikuwa wa-
mesimama karibu na nyumba
tuliyokuwamo, wakiwa wame-
tumwa kutoka Kaisaria kuja
kwangu.[c] **12** Kwa hiyo roho[d]
ikaniambia niende pamoja nao,
bila kuwa na shaka hata kido-
go. Lakini ndugu sita hawa pia
walikwenda pamoja nami, nasi
tukaingia ndani ya nyumba ya
mwanamume huyo.[e]

13 "Alitueleza jinsi alivyo-
mwona malaika amesimama ka-
tika nyumba yake na kusema,
'Tuma watu waende Yopa wa-
kamwite Simoni anayeitwa Pe-
tro,[f] **14** naye atasema nawe
mambo ambayo yatakuwezesha
wewe na watu wote wa nyumba
yako kuokolewa.'[g] **15** Lakini
nilipoanza kusema, roho taka-
tifu ikawaangukia kama vile ili-
vyoanguka pia juu yetu mwa-
nzoni.[h] **16** Ndipo nikayaku-
mbuka maneno ya Bwana, jinsi
alivyokuwa akisema, 'Yohana
alibatiza kwa maji,[i] lakini ni-
nyi mtabatizwa kwa roho taka-
tifu.'[j] **17** Kwa hiyo, ikiwa Mu-
ngu aliwapa hao zawadi ileile
ya bure kama vile alivyotupa
sisi pia ambao tumemwamini
Bwana Yesu Kristo,[k] mimi ni
nani hata niweze kumzuia Mu-
ngu?"[l]

18 Basi waliposikia mambo
hayo, wakakubali kimyaki-
mya,[m] nao wakamtukuza Mu-
ngu,[n] wakisema: "Kwa hiyo,
basi, Mungu ameruhusu toba
kwa kusudi la uzima kwa watu
wa mataifa pia."[o]

SURA 10
a Mdo 2:4
Mdo 19:6
b Mt 3:11
Mdo 8:36
Mdo 11:17
c Mt 16:19
Mdo 2:38
Mdo 19:5

SURA 11
d Zek 2:11
Lu 2:32
Mdo 14:27
e Mdo 10:45
Ga 2:12
f Mdo 10:12
g Mdo 10:13
h Eze 4:14
Mt 15:11
Mdo 10:14

Safu ya 2
a Mdo 15:9
b Mdo 10:16
c Mdo 10:17
d Yoh 16:13
Mdo 10:19
e Mdo 10:23
Mdo 15:7
f Mdo 10:30
g Mdo 16:30
h Mdo 2:4
i Mt 3:11
Mk 1:8
Lu 3:16
Mdo 1:5
j Isa 44:3
Yoe 2:28
Yoh 1:33
Mdo 2:17
k Mdo 15:8
Ga 3:2
l Da 4:35
Mdo 10:47
m Mdo 21:14
n Lu 2:20
Mdo 13:48
Mdo 14:27
o Isa 11:10
Mdo 17:30
Mdo 20:21
Ro 10:12
Ro 15:9

19 Kwa sababu hiyo wale waliokuwa wametawanywa[a] na dhiki iliyotokea kwa sababu ya Stefano wakapita kwenda mpaka Foinike[b] na Kipro[c] na Antiokia, lakini hawakusema lile neno kwa yeyote ila kwa Wayahudi tu.[d] **20** Hata hivyo, kati yao kulikuwa na wanaume fulani wa Kipro na Kirene waliokuja Antiokia na kuanza kuongea na watu wenye kusema Kigiriki,[e] wakitangaza habari njema ya Bwana Yesu.[f] **21** Zaidi ya hayo, mkono wa Yehova[g] ulikuwa pamoja nao, na hesabu kubwa ya waliopata kuwa waamini wakageuka kumwelekea Bwana.[h]

22 Kutaniko lililokuwa katika Yerusalemu likasikia juu yao, nao wakamtuma Barnaba[i] mpaka Antiokia. **23** Alipofika na kuziona fadhili zisizostahiliwa[j] za Mungu, akashangilia[k] na kuanza kuwatia wote moyo waendelee katika Bwana wakiwa na azimio la moyoni;[l] **24** kwa maana alikuwa mwanamume mwema na mwenye kujaa roho takatifu na imani. Na umati mkubwa ukaongezwa kwa Bwana.[m] **25** Kwa hiyo akaenda zake mpaka Tarso[n] ili kumtafuta Sauli[o] **26** na, baada ya kumpata, akamleta Antiokia. Hivyo ikatukia kwamba kwa mwaka mzima wakakusanyika pamoja nao katika kutaniko na kufundisha umati mkubwa, na kule Antiokia ndipo ambapo kwa mara ya kwanza wanafunzi kwa uongozi wa kimungu waliitwa Wakristo.[p]

27 Basi katika siku hizo manabii[q] walishuka kutoka Yerusalemu mpaka Antiokia. **28** Mmoja kati yao anayeitwa jina Agabo[a] akasimama na kuonyesha kupitia roho kwamba njaa kali ilikuwa karibu kuja juu ya dunia nzima inayokaliwa;[b] ambayo, kama ilivyo, ilitukia wakati wa Klaudio. **29** Kwa hiyo wanafunzi wakaamua, kila mmoja kwa kadiri ambayo yeyote angeweza kutoa,[c] wafanye huduma ya kupeleka misaada[d] kwa akina ndugu waliokuwa wakikaa Yudea; **30** nao wakafanya hivyo, wakaipeleka kwa wanaume wazee kwa mkono wa Barnaba na Sauli.[e]

12 Karibu na wakati huo Mfalme Herode alitumia mikono yake kuwatendea vibaya[f] baadhi ya wale wa kutaniko. **2** Alimuua kwa upanga[g] Yakobo ndugu ya Yohana.[h] **3** Alipoona kuwa jambo hilo limewapendeza Wayahudi,[i] akamkamata Petro pia. (Ikawa kwamba hizo zilikuwa siku za keki zisizo na chachu.)[j] **4** Na alipomkamata, akamweka gerezani,[k] akamkabidhi kwenye zamu nne za askari-jeshi wanne kila moja ili kumlinda, kwa kuwa alikusudia kumleta mbele ya watu baada ya pasaka.[l] **5** Kwa hiyo Petro alikuwa gerezani; lakini kutaniko lilikuwa likisali[m] kwa Mungu kwa juhudi nyingi kwa ajili yake.

6 Sasa Herode alipokuwa karibu kumtoa, usiku huo Petro alikuwa amelala akiwa amefungwa kwa minyororo miwili katikati ya askari-jeshi wawili, na walinzi mbele ya mlango walikuwa wakililinda gereza. **7** Lakini, tazama! malaika wa Yehova akasimama[n] kando, na nuru ikang’aa katika chumba cha gereza. Akampiga Petro ubavuni, akamwamsha,[o] akise-

SURA 11

a Mdo 8:1
b Mdo 21:2
c Mdo 21:3
d Mt 10:6
e Mdo 6:1
Mdo 9:29
f Mk 13:10
Efe 3:8
g Lu 1:66
h Mdo 2:47
Mdo 9:35
i Mdo 4:36
j Ebr 12:15
k 3Yo 4
l Mdo 13:43
Mdo 14:22
m Mdo 2:47
Mdo 4:4
Mdo 5:14
Mdo 9:31
n Mdo 21:39
o Mdo 9:30
p Mdo 9:2
q Mdo 13:1
Mdo 15:32
1Ko 12:28
Efe 4:11

Safu ya 2

a Mdo 21:10
b Mt 24:7
Lu 4:25
c 2Ko 8:12
d Law 25:35
Met 3:27
Mdo 24:17
Ro 15:26
1Ko 16:1
Ga 2:10
e Mdo 12:25
Ga 2:1

SURA 12

f Yoh 15:20
Mdo 4:3
g Mt 20:23
Lu 11:49
h Mt 4:21
i Mdo 24:27
j Kut 12:15
Kut 23:15
Law 23:6
k Lu 21:12
Mdo 5:18
l Kut 12:11
m 2Ko 1:11
Efe 6:18
1Th 5:17
Yak 5:16
n Zb 34:7
Ebr 1:14
o 1Fa 19:7

ma: “Amka upesi!” Na minyoro-
ro yake ikaanguka[a] kutoka kwe-
nye mikono yake. **8** Malaika[b]
akamwambia: “Jifunge kiuno
na uvae viatu vyako.” Akafa-
nya hivyo. Mwishowe akamwa-
mbia: “Vaa vazi[c] lako la nje
uendelee kunifuata.” **9** Naye
akatoka na kuendelea kumfua-
ta, lakini hakujua kwamba lililo-
kuwa likitukia kupitia malaika
lilikuwa halisi. Kwa kweli, ali-
dhani alikuwa akiona maono.[d]
10 Wakampita askari-mlinzi
wa kwanza na wa pili wakafika
kwenye lango la chuma linaloe-
lekea jijini, nalo likafunguka le-
nyewe mbele yao.[e] Na baada
ya kutoka wakapita katika ba-
rabara moja, na mara malai-
ka akamwacha. **11** Na Petro
akarudiwa na fahamu, akase-
ma: “Sasa ninajua hakika kwa-
mba Yehova alimtuma[f] malaika
wake na kunikomboa[g] kutoka
mkononi mwa Herode na kuto-
ka katika yote ambayo Wayahu-
di wote walikuwa wakitarajia.”

12 Na baada ya kufikiria jam-
bo hilo, akaenda kwenye
nyumba ya Maria mama ya Yo-
hana aliyeitwa Marko,[h] amba-
mo watu wengi walikuwa
wamekusanyika na wakisali.
13 Alipopiga hodi kwenye mla-
ngo wa njia ya lango, kijaka-
zi anayeitwa Roda akaja kujibu,
14 na, alipoitambua sauti ya Pe-
tro, hakulifungua lango kwa sa-
babu ya shangwe, bali akaki-
mbia ndani na kueleza kwa-
mba Petro alikuwa amesimama
mbele ya njia ya lango. **15** Wa-
kamwambia: “Una wazimu.”
Lakini akasisitiza kwa nguvu
ndivyo ilivyokuwa. Wakaanza
kusema: “Ni malaika wake.”[i]
16 Lakini Petro akakaa hapo
akibisha mlango. Walipofu-
ngua, wakamwona nao waka-
shangaa. **17** Lakini akawa-
pungia[a] mkono wanyamaze na
kuwaambia kirefu jinsi Yeho-
va alivyomtoa gerezani, naye
akasema: “Waambieni Yakobo[b]
na akina ndugu mambo haya.”
Ndipo akatoka, akasafiri kwe-
nda mahali pengine.

18 Basi, mchana ulipofika,[c]
kulikuwa na msukosuko usio
mdogo kati ya askari-jeshi ku-
husu ni jambo gani kwa kwe-
li lililokuwa limempata Petro.
19 Herode[d] akamtafuta kwa
bidii na, alipokosa kumpata,
akawahoji walinzi na kuwaa-
muru wapelekwe kuadhibiwa;[e]
naye akashuka kwenda Yudea
mpaka Kaisaria na kukaa huko
kwa muda fulani.

20 Sasa yeye alitaka kupiga-
na na watu wa Tiro na wa Si-
doni. Kwa hiyo wakamjia kwa
umoja na, baada ya kumsha-
wishi Blasto, aliyekuwa msi-
mamizi wa chumba cha kula-
la cha mfalme, wakaanza ku-
toa ombi la kutaka amani, kwa
sababu nchi yao iligawiwa cha-
kula[f] kutoka katika kile cha
mfalme. **21** Lakini siku fu-
lani iliyowekwa Herode aka-
jivika vazi la kifalme na ku-
keti juu ya kiti cha hukumu
na kuanza kuwatolea hotuba
ya watu wote. **22** Nao watu
waliokusanyika wakaanza ku-
paaza sauti: “Ni sauti ya mu-
ngu, wala si ya mwanadamu!”[g]
23 Papo hapo malaika wa Yeho-
va akampiga,[h] kwa sababu ha-
kumpa Mungu utukufu;[i] naye
akaliwa na wadudu akakata
pumzi.

24 Lakini neno[j] la Yehova li-
kaendelea kukua na kuenea.[k]

SURA 12

a Mdo 16:26

b Mdo 5:19

c Mk 10:50

d Mdo 11:5

e Mdo 16:26

f Zb 34:7
Da 3:28
Da 6:22
Ebr 1:14

g 2Pe 2:9

h Mdo 13:5
Mdo 15:37
Kol 4:10

i Mwa 48:16
Mt 18:10

Safu ya 2

a Mdo 13:16
Mdo 19:33

b Mt 13:55
Mdo 15:13
Mdo 21:18
1Ko 15:7
Ga 1:19
Ga 2:9

c Mdo 5:21

d Mdo 12:6

e Mdo 16:27

f 1Fa 5:9
Eze 27:17

g Eze 28:2
Yud 16

h 2Sa 24:17
2Nya 32:21

i Isa 42:8
1Ko 1:29

j Isa 55:11
Mdo 6:7
Mdo 19:20

k Kol 1:6

25 Naye Barnaba[a] na Sauli, baada ya kutimiza kikamili ile huduma ya misaada[b] katika Yerusalemu, wakarudi na kumchukua pamoja nao Yohana,[c] aliyeitwa Marko.

13 Basi katika Antiokia kulikuwa na manabii[d] na walimu katika kutaniko la mahali hapo, Barnaba na vilevile Simioni aliyeitwa Nigeri, na Lukio[e] wa Kirene, na Manaeni aliyeelimishwa pamoja na Herode mtawala wa wilaya, na Sauli. **2** Walipokuwa wakimhudumia[f] Yehova hadharani na kufunga, roho takatifu ikasema: "Kati ya watu wote wekeni kando Barnaba na Sauli[g] kwa ajili yangu kwa kazi ambayo nimewaitia wao." **3** Ndipo wakafunga na kusali na kuweka mikono[h] yao juu yao, wakawaacha waende zao.

4 Basi watu hawa, waliotumwa na roho takatifu, wakashuka kwenda Seleukia, na kutoka huko wakasafiri kwa mashua kwenda Kipro. **5** Na walipofika Salami wakaanza kulitangaza neno la Mungu katika masinagogi ya Wayahudi. Pia walikuwa na Yohana[i] akiwatumikia.

6 Walipokuwa wamepita katika kisiwa chote mpaka Pafo, wakakutana na mwanamume fulani, mlozi, nabii wa uwongo,[j] Myahudi ambaye jina lake lilikuwa Bar-Yesu, **7** naye alikuwa pamoja na liwali Sergio Paulo, mwanamume mwenye akili. Akawaita Barnaba na Sauli, naye mtu huyu akataka kulisikia neno la Mungu. **8** Lakini Elima mlozi (hivyo, kwa kweli, ndivyo jina lake linavyotafsiriwa) akaanza kuwapinga,[k] akitafuta kumgeuzia mbali yule liwali kutoka kwenye ile imani. **9** Sauli, ambaye pia ni Paulo, akiwa amejaa roho takatifu, akamtazama **10** na kusema: "Ewe mtu mwenye kujaa kila namna ya upunjaji na kila namna ya ulaghai, wewe mwana wa Ibilisi, wewe adui wa kila jambo la uadilifu, je, hutaacha kuzipotoa njia zilizo sawa za Yehova?[a] **11** Hivyo, basi, tazama! mkono wa Yehova uko juu yako wewe, nawe utakuwa kipofu, usiweze kuiona nuru ya jua kwa kipindi fulani." Mara moja ukungu mzito na giza vikamwangukia, naye akazunguka akitafuta watu wa kumwongoza wakiwa wamemshika mkono.[b] **12** Ndipo yule liwali,[c] alipoona jambo lililokuwa limetukia, akawa mwamini, kwa kuwa alistaajabishwa na fundisho la Yehova.

13 Hao watu, pamoja na Paulo, sasa wakasafiri baharini kutoka Pafo na kufika Perga katika Pamfilia.[d] Lakini Yohana[e] akawaacha na kurudi[f] Yerusalemu. **14** Hata hivyo, wao wakaendelea kutoka Perga na kuja Antiokia katika Pisidia nao wakaingia ndani ya sinagogi[g] siku ya sabato, wakaketi. **15** Baada ya kusoma Sheria[h] na Manabii mbele ya watu wote maofisa-wasimamizi[i] wa sinagogi wakawatuma watu kwao, wakisema: "Wanaume, akina ndugu, ikiwa kuna neno lolote la kitia moyo mlilo nalo kwa ajili ya watu, lisemeni." **16** Kwa hiyo Paulo akasimama, akapunga[j] mkono wake, akasema:

"Wanaume, Waisraeli na ninyi wengine ambao mnamwo-

SURA 12
a Mdo 4:36
b Mdo 11:29
c Mdo 13:5
Mdo 15:37

SURA 13
d Mdo 11:27
Mdo 15:32
1Ko 12:28
Efe 4:11
e Mdo 11:20
f Efe 3:7
1Ti 2:7
g Mdo 9:15
Ebr 5:4
h Mdo 14:23
1Ti 4:14
2Ti 1:6
i Mdo 12:25
j Mt 24:24
k 2Ti 3:8

Safu ya 2
a Mt 13:38
Yoh 8:44
1Yo 3:8
b Mdo 9:8
c Mdo 19:38
d Mdo 15:38
e Mdo 12:12
f Mdo 15:38
g Mdo 16:13
Mdo 17:2
Mdo 18:4
Mdo 19:8
h Mdo 15:21
i Mk 5:22
j Mdo 12:17
Mdo 21:40
Mdo 26:1

gopa Mungu, sikieni.[a] **17** Mungu wa watu hawa Israeli aliwachagua mababu zetu, naye akawainua watu hao walipokuwa wakikaa katika nchi ya kigeni katika nchi ya Misri na kuwatoa katika hiyo kwa mkono ulioinuliwa.[b] **18** Na kwa kipindi cha karibu miaka 40[c] akavumilia jinsi walivyotenda nyikani. **19** Baada ya kuyaangamiza mataifa saba katika nchi ya Kanaani, aligawanya nchi yao kwa kura:[d] **20** yote haya wakati wa karibu miaka 450.

"Na baada ya mambo hayo aliwapa waamuzi mpaka nabii Samweli.[e] **21** Lakini tangu hapo na kuendelea wakadai mfalme,[f] na Mungu akawapa Sauli mwana wa Kishi, mwanamume wa kabila la Benyamini,[g] kwa miaka 40. **22** Na baada ya kumwondoa huyo,[h] akawainulia Daudi kuwa mfalme,[i] ambaye alitoa ushahidi kumhusu na kusema, 'Nimemwona Daudi mwana wa Yese,[j] mtu anayekubalika kwa moyo wangu,[k] atakayefanya mambo yote ambayo ninatamani.'[l] **23** Kutoka katika uzao[m] wa mwanamume huyu kulingana na ahadi yake Mungu ameletea Israeli mwokozi,[n] Yesu, **24** baada ya Yohana,[o] kabla ya kuingia kwake Huyo,[p] akiwa amekwisha kuhubiri hadharani kwa watu wote wa Israeli ubatizo unaoonyesha toba. **25** Lakini Yohana alipokuwa akitimiza mwendo wake, akawa akisema 'Mnadhani mimi ni nani? Mimi si yeye. Lakini, tazameni! mmoja anakuja baada yangu ambaye viatu vya miguu yake mimi sistahili kuvifungua.'[q]

SURA 13

a Mdo 13:26
b Kut 6:6
Kut 14:8
Kum 7:6
c Kut 16:35
Hes 14:34
Kum 2:7
d Kum 7:1
Yos 14:2
e Amu 2:16
1Sa 3:20
f 1Sa 8:5
g 1Sa 10:21
1Sa 11:15
h Ho 13:11
i 1Sa 16:12
2Sa 2:4
Zb 89:20
j 1Sa 16:1
k 1Sa 13:14
l Isa 44:28
m 2Sa 7:12
Isa 11:1
n Lu 1:32
Lu 1:69
Ro 11:26
o Mt 3:1
Lu 16:16
p Mt 1:21
q Mt 3:11
Lu 3:16

Safu ya 2

a Mt 10:6
Lu 24:47
b Yoh 16:3
Mdo 3:17
c Zb 22:16
Zb 41:9
Isa 53:7
Zek 11:12
d Mt 26:60
Lu 23:15
Yoh 19:4
e Mt 27:22
Yoh 19:15
f Lu 18:31
Yoh 19:36
g Yoh 19:40
h Mt 27:60
i Mt 28:6
Mdo 2:24
j Mt 28:16
Mdo 1:3
Mdo 3:15
1Ko 15:6
k Mwa 12:3
Mdo 13:23
Ro 4:13
l Ro 1:4
m Zb 2:7
Ebr 1:5
Ebr 5:5
n Isa 55:3

26 "Wanaume, akina ndugu, ninyi wana wa ukoo wa Abrahamu na wale wengine kati yenu ambao mnamwogopa Mungu, neno la wokovu huu limeletwa kwetu sisi.[a] **27** Kwa maana wakaaji wa Yerusalemu na watawala wao hawakumjua Huyu,[b] bali, walipokuwa wakitenda wakiwa waamuzi, walitimiza mambo yaliyosemwa na Manabii,[c] mambo ambayo husomwa kwa sauti kubwa kila Sabato, **28** na, ijapokuwa hawakupata sababu yoyote ya kumuua[d] walidai kwa Pilato kwamba auawe.[e] **29** Basi, walipokuwa wametimiza mambo yote yaliyoandikwa juu yake,[f] walimshusha chini kutoka kwenye mti[g] na kumlaza katika kaburi.[h] **30** Lakini Mungu akamfufua kutoka kwa wafu;[i] **31** na kwa siku nyingi akaonekana kwa wale ambao walikuwa wamepanda kwenda pamoja naye kutoka Galilaya mpaka Yerusalemu, ambao sasa ni mashahidi wake kwa watu.[j]

32 "Na kwa hiyo sisi tunawatangazia ninyi habari njema juu ya ahadi iliyotolewa kwa mababu,[k] **33** kwamba Mungu ameitimiza kabisa kwetu sisi tulio watoto wao kwa kuwa alimfufua Yesu;[l] hata kama vile ambavyo imeandikwa katika zaburi ya pili, 'Wewe ni mwanangu, mimi nimekuwa Baba yako leo.'[m] **34** Na jambo hilo la kwamba yeye alimfufua kutoka kwa wafu akikusudiwa asirudi tena kwenye uharibifu, yeye amelisema katika njia hii, 'Nitawapa ninyi fadhili zenye upendo kwa Daudi ambazo ni za uaminifu.'[n] **35** Kwa sababu hiyo anasema pia katika

zaburi nyingine, ‘Hutamruhusu mshikamanifu wako aone uharibifu.’[a] **36** Kwa maana Daudi,[b] kwa upande mmoja, alitumikia mapenzi kamili ya Mungu katika kizazi chake mwenyewe na kulala katika kifo na alilazwa pamoja na mababu zake na kuona uharibifu.[c] **37** Kwa upande mwingine, yule ambaye Mungu alimfufua hakuona uharibifu.[d]

38 “Kwa hiyo acheni ijulikane kwenu, akina ndugu, kwamba kupitia Huyo msamaha wa dhambi unatangazwa kwenu;[e] **39** na kwamba kutokana na mambo yote ambayo ninyi hamngeweza kutangazwa kuwa bila hatia kwa njia ya sheria ya Musa,[f] kila mtu anayeamini anatangazwa kuwa bila hatia kwa njia ya Huyu.[g] **40** Kwa hiyo hakikisheni kwamba yale yaliyosemwa katika Manabii hayaji juu yenu, **41** ‘Oneni, ninyi wenye kudharau, mstaajabie, na mtoweke, kwa sababu ninafanya tendo katika siku zenu, tendo ambalo hamtaliamini hata kidogo hata yeyote akiwaeleza kirefu.’”[h]

42 Basi walipokuwa wakitoka, watu wakaanza kusihi waambiwe mambo hayo siku ya sabato inayofuata.[i] **43** Kusanyiko la sinagogi lilipomalizika, wengi kati ya Wayahudi na kati ya wageuzwa-imani waliomwabudu Mungu wakawafuata Paulo na Barnaba,[j] ambao walisema nao na kuanza kuwahimiza[k] waendelee kubaki katika fadhili zisizostahiliwa za Mungu.[l]

44 Siku ya Sabato iliyofuata karibu jiji lote lilikusanyika pamoja kulisikia neno la Yehova.[m] **45** Wayahudi walipoona umati, walijawa na wivu[a] na kuanza kuyapinga kwa kukufuru mambo yaliyokuwa yakisemwa na Paulo.[b] **46** Na kwa hiyo, wakiongea kwa ujasiri, Paulo na Barnaba wakasema: “Ilikuwa lazima neno la Mungu lihubiriwe kwenu kwanza.[c] Kwa kuwa mnalisukumia mbali[d] kutoka kwenu na hamjioni kuwa mnastahili uzima wa milele, tazameni! tunawageukia mataifa.[e] **47** Kwa kweli, Yehova ameweka amri juu yetu kwa maneno haya, ‘Nimewaweka ninyi kuwa nuru ya mataifa,[f] ili muwe wokovu mpaka sehemu ya mwisho ya dunia.’”[g]

48 Wale wa mataifa waliposikia jambo hilo, wakaanza kushangilia na kulitukuza neno la Yehova,[h] na wale wote waliokuwa na mwelekeo unaofaa kwa ajili ya uzima wa milele wakawa waamini.[i] **49** Zaidi ya hayo, neno la Yehova likaendelea kupelekwa kotekote katika nchi yote.[j] **50** Lakini Wayahudi[k] wakawachochea wanawake wenye kusifika waliomwabudu Mungu na wakuu wa jiji, nao wakazusha mateso[l] juu ya Paulo na Barnaba na kuwatupa nje ya mipaka yao. **51** Hawa wakawakung’utia mavumbi kutoka miguuni pao[m] na kwenda Ikoniamu. **52** Na wanafunzi wakaendelea kujawa na shangwe[n] na roho takatifu.

14 Basi katika Ikoniamu[o] wakaingia pamoja katika sinagogi[p] la Wayahudi na kusema kwa namna ambayo iliufanya umati mkubwa wa Wayahudi na pia Wagiriki[q] kuwa waamini. **2** Lakini Wayahudi ambao hawakuamini wakachochea[r] na

SURA 13

a Zb 16:10
Mdo 2:31
b Mdo 2:34
c 1Fa 2:10
Mdo 2:29
d Mdo 2:27
e Da 9:24
Lu 24:47
Mdo 5:31
Mdo 10:43
f Ro 8:3
Ebr 7:19
Ebr 10:1
g Isa 53:11
Ro 3:28
Ro 5:18
h Hab 1:5
i Mdo 18:4
j Mdo 17:4
k Mdo 14:22
l Mdo 11:23
Tit 2:11
m Mdo 12:24

Safu ya 2

a Met 27:4
b Mdo 14:2
Mdo 17:5
c Mt 10:6
Mdo 3:26
Ro 1:16
d Mt 22:8
Lu 7:30
e Isa 55:5
Lu 2:32
Mdo 18:6
Ro 10:19
f Isa 42:6
g Isa 49:6
Mdo 1:8
h Isa 39:5
Isa 66:5
Mdo 11:18
2Th 1:12
i Ro 8:29
j Mdo 15:36
k Mdo 14:2
Mdo 14:19
l Mt 23:34
Mdo 17:5
2Ti 3:11
m Mt 10:14
Lu 9:5
Mdo 18:6
n Mt 5:12
1Th 1:6

SURA 14

o 2Ti 3:11
p Mdo 13:5
q Mdo 17:4
r Mdo 13:45

kuwa na uvutano mbaya juu ya nafsi za watu wa mataifa dhidi ya akina ndugu.[a] **3** Kwa hiyo wakatumia muda mrefu wakisema kwa ujasiri kwa mamlaka ya Yehova, aliyetoa ushahidi kuhusu neno la fadhili zake zisizostahiliwa kwa kuruhusu ishara na mambo ya ajabu kutukia kupitia kwa mikono yao.[b] **4** Hata hivyo, umati wa jiji ukagawanyika, na baadhi yao walikuwa upande wa Wayahudi lakini wengine upande wa mitume. **5** Basi watu wa mataifa na pia Wayahudi pamoja na watawala wao walipojaribu kwa jeuri kuwatendea kwa dharau na kuwatupia mawe,[c] **6** wao, walipojulishwa jambo hilo, wakakimbilia[d] majiji ya Likaonia, Listra na Derbe na nchi yenye kuzunguka; **7** na huko wakaendelea kutangaza habari njema.[e]

8 Sasa katika Listra mwanamume fulani aliyekuwa amelemaa miguu alikuwa ameketi, kilema tangu alipokuwa katika tumbo la uzazi la mama yake,[f] naye alikuwa hajatembea kamwe. **9** Mtu huyo alikuwa akimsikiliza Paulo akisema, ambaye, alipomtazama na kuona kwamba ana imani[g] ya kuponywa, **10** akasema kwa sauti kubwa: "Simama wima kwa miguu yako." Naye akaruka na kuanza kutembea.[h] **11** Na umati, walipoona jambo ambalo Paulo alikuwa amefanya, wakapaaza sauti, wakisema katika lugha ya Kilikaonia: "Miungu[i] imekuwa kama binadamu nayo imeshuka kwetu!" **12** Naye Barnaba wakamwita Zeu, lakini Paulo wakamwita Herme, kwa kuwa ndiye aliyekuwa akiongoza katika kusema. **13** Na kuhani wa Zeu, ambaye hekalu lake lilikuwa mbele ya jiji, akaleta ng'ombedume na shada za maua kwenye malango naye alikuwa anataka kutoa dhabihu[a] pamoja na umati.

14 Hata hivyo, mitume Barnaba na Paulo waliposikia jambo hilo, wakayararua mavazi yao ya nje na kuruka ndani ya umati, wakipaaza sauti **15** na kusema: "Wanaume, kwa nini mnafanya mambo haya? Sisi pia ni wanadamu[b] tulio na udhaifu[c] uleule kama ninyi, nasi tunawatangazia ninyi habari njema, ili mgeuke kutoka kwa mambo haya ya bure[d] mpate kumjia Mungu aliye hai,[e] aliyefanya mbingu[f] na dunia na bahari na vitu vyote vilivyomo. **16** Katika vizazi vilivyopita yeye aliwaruhusu mataifa yote waendelee kutembea katika njia zao,[g] **17** ijapokuwa, kwa kweli, hakujiacha mwenyewe bila ushahidi kwa kuwa alitenda mema,[h] akiwapa ninyi mvua[i] kutoka mbinguni na majira yenye kuzaa matunda, akijaza mioyo yenu kikamili kwa chakula na uchangamfu."[j] **18** Na bado kwa kusema mambo haya wakauzuia umati kwa shida, wasiwatolee dhabihu.

19 Lakini Wayahudi wakafika kutoka Antiokia na Ikoniamu wakaushawishi umati,[k] nao wakampiga Paulo kwa mawe na kumkokota nje ya jiji, wakiwazia alikuwa amekufa.[l] **20** Hata hivyo, wanafunzi walipomzunguka, akasimama na kuingia ndani ya jiji. Na siku iliyofuata akaondoka pamoja na Barnaba kwenda

SURA 14

a Ro 15:31

b Mdo 5:12
Mdo 19:11
Ebr 2:4

c Mdo 14:19
1Th 2:2
2Ti 3:11

d Mt 10:23

e 1Ko 1:17

f Mdo 3:2

g Mt 9:28

h Isa 35:6
Mdo 3:8

i Mdo 12:22
Mdo 28:6

Safu ya 2

a Da 2:46

b Mdo 10:26

c Yak 5:17

d Kum 32:21
1Sa 12:21
Yer 10:15

e 1Th 1:9

f Mwa 1:1
Kut 20:11
Zb 33:6
Zb 146:6
Mdo 4:24

g Kum 18:14
Mdo 17:30

h Mdo 17:27
Ro 1:20

i Zb 65:10
Zb 147:8
Yer 5:24
Mt 5:45

j Zb 145:16

k Mdo 17:13

l 2Ko 6:9
2Ko 11:25
2Ti 3:11

Derbe.[a] **21** Na baada ya kulitangazia jiji hilo habari njema na kufanya wanafunzi[b] wengi, wakarudi Listra na Ikoniamu na Antiokia, **22** wakizitia nguvu nafsi za wanafunzi,[c] wakiwatia moyo kubaki katika imani na kusema: "Lazima tuingie katika ufalme wa Mungu kupitia dhiki nyingi."[d] **23** Zaidi ya hayo, wakawaweka rasmi wanaume wazee[e] kwa ajili yao katika kila kutaniko, wakatoa sala pamoja na kufunga,[f] na kuwakabidhi kwa Yehova[g] ambaye walikuwa wamemwamini.

24 Nao wakapita katika Pisidia na kuingia Pamfilia,[h] **25** na, baada ya kulisema neno katika Perga, wakashuka kwenda Atalia. **26** Na kutoka huko wakasafiri kwenda Antiokia,[i] walikokuwa wamekabidhiwa kwenye fadhili zisizostahiliwa za Mungu kwa ajili ya kazi waliyokuwa wameifanya kikamili.[j]

27 Walipokuwa wamefika na wakiwa wamelikusanya kutaniko pamoja, wakaeleza mambo mengi[k] ambayo Mungu alikuwa amefanya kupitia kwao, na kwamba alikuwa amewafungulia mataifa mlango wa kuingia katika imani.[l] **28** Kwa hiyo wakatumia muda usio mdogo wakiwa pamoja na wanafunzi.

15 Na watu fulani wakashuka kutoka Yudea[m] na kuanza kuwafundisha ndugu: "Msipotahiriwa[n] kulingana na desturi ya Musa,[o] hamwezi kuokolewa." **2** Lakini kulipokuwa kumetokea mtengano usio mdogo na bishano kati ya Paulo na Barnaba pamoja nao, wakapanga Paulo na Barnaba na wengine kati yao wapande kwenda kwa mitume na wanaume wazee katika Yerusalemu[a] kuhusu bishano hilo.

3 Basi, baada ya kusindikizwa na kutaniko,[b] watu hao wakaenda zao wakipitia Foinike na pia Samaria, wakieleza kirefu kugeuka kwa watu wa mataifa,[c] nao walikuwa wakitokeza shangwe kubwa kwa akina ndugu wote.[d] **4** Walipofika Yerusalemu walikaribishwa kwa fadhili[e] na kutaniko na mitume na wanaume wazee, nao wakaeleza mambo mengi ambayo Mungu alikuwa ameyafanya kupitia kwao.[f] **5** Lakini, baadhi ya wale wa madhehebu ya Mafarisayo waliokuwa wameamini wakasimama kutoka kwenye viti vyao na kusema: "Ni lazima kuwatahiri[g] na kuwaamuru washike sheria ya Musa."[h]

6 Na mitume na wanaume wazee wakakusanyika pamoja ili waliangalie jambo hilo.[i] **7** Basi bishano[j] kubwa lilipokuwa limetukia, Petro akasimama na kuwaambia: "Wanaume, akina ndugu, ninyi mnajua vema kwamba tangu siku za zamani Mungu alichagua kati yenu kwamba kupitia kinywa changu watu wa mataifa wasikie neno la habari njema na kuamini;[k] **8** na Mungu, anayeujua moyo,[l] alitoa ushahidi kwa kuwapa wao roho takatifu,[m] kama vile alivyotupa sisi pia. **9** Naye hakufanya tofauti hata kidogo kati yetu na wao,[n] bali aliisafisha mioyo yao kwa imani.[o] **10** Kwa hiyo, sasa kwa nini mnamjaribu Mungu kwa kuweka juu ya shingo za wanafunzi nira[p] ambayo ma-

SURA 14
a Mdo 16:1
b Mt 28:19
c Mdo 11:23
d Mt 10:38
Yoh 15:19
Ro 8:17
1Th 3:4
e Tit 1:5
f Mdo 13:3
g Mdo 20:32
h Mdo 13:13
i Mdo 13:1
j 1Ko 15:10
k Mdo 15:4
Mdo 21:19
l Mdo 11:18
1Ko 16:9

SURA 15
m Ga 2:12
n Ga 5:2
o Mwa 17:10
Kut 12:48
Law 12:3

Safu ya 2
a Mdo 11:30
Mdo 16:4
Ga 2:1
b Ro 15:24
1Ko 16:6
c Mdo 13:4
Mdo 14:27
d Mdo 11:18
e Mdo 21:17
f Mdo 21:19
g Mdo 11:2
h Kut 12:48
i Met 13:10
Met 15:22
j Mk 9:16
Mdo 15:2
k Mdo 10:34
Mdo 11:17
l 1Nya 28:9
Yer 11:20
Mdo 1:24
m Mdo 10:44
Mdo 11:15
n Ga 3:28
o Ga 2:16
1Pe 1:22
p Ga 5:1

babu zetu wala sisi hatukuweza
kubeba?[a] **11** Kinyume chake,
sisi tunaamini kwamba tuta-
okolewa kupitia fadhili zisizo-
stahiliwa[b] za Bwana Yesu ka-
tika njia ileile kama watu hao
pia."[c]

12 Ndipo umati mzima uka-
nyamaza, nao wakaanza kuwa-
sikiliza Barnaba na Paulo waki-
eleza ishara nyingi na mambo
mengi ya ajabu ambayo Mungu
alifanya kupitia kwao katikati
ya mataifa.[d] **13** Walipomali-
za kusema, Yakobo akajibu, aki-
sema: "Wanaume, akina ndugu,
nisikieni.[e] **14** Simioni[f] amee-
leza kikamili jinsi Mungu kwa
mara ya kwanza alivyoeleke-
za uangalifu wake kwa mata-
ifa ili achukue kutoka kwao
watu kwa ajili ya jina lake.[g]
15 Na maneno ya Manabii ya-
nakubaliana na jambo hili,
kama vile ambavyo imeandi-
kwa, **16** 'Baada ya mambo
hayo nitarudi na kukijenga
upya kibanda cha Daudi amba-
cho kimeanguka chini; nami
nitayajenga upya mabomoko
yake na kukisimamisha tena,[h]
17 ili watu wanaobaki wamta-
fute Yehova kwa bidii, pamoja
na watu wa mataifa yote, watu
wanaoitwa kwa jina langu, ase-
ma Yehova, anayefanya mambo
haya,[i] **18** yanayojulikana tan-
gu zamani za kale.'[j] **19** Kwa
hiyo nimeamua kutowataabi-
sha wale wa kutoka katika ma-
taifa wanaomgeukia Mungu,[k]
20 bali kuwaandikia wajiepu-
she na vitu vilivyochafuliwa na
sanamu,[l] na uasherati,[m] na kile
kilichonyongwa,[n] na damu.[o]
21 Kwa maana tangu nyaka-
ti za kale katika jiji baada ya
jiji Musa amekuwa na wale wa-

SURA 15

a Ga 3:10
b Isa 53:11
Yoh 1:17
Ga 2:16
c Mt 20:28
d Ro 15:19
e Mdo 12:17
f Mdo 11:13
2Pe 1:1
g Isa 55:5
1Pe 2:9
h Amo 9:11
i Amo 9:12
j Isa 45:21
k Mdo 15:10
l Mwa 35:2
Kut 20:3
Eze 20:30
1Ko 8:7
1Ko 10:14
m 1Ko 6:9
Kol 3:5
1Th 4:3
n Law 17:13
o Mwa 9:4
Law 3:17
Law 7:26
Law 17:10
Law 19:26
Kum 12:23
Kum 15:23
1Sa 14:32

Safu ya 2

a Mdo 13:15
2Ko 3:15
b Mdo 1:23
c Mdo 11:26
d Ga 1:21
e Mdo 15:1
f Ga 2:4
Tit 1:10
g Mdo 1:14
h 2Pe 3:15
i Mdo 13:50
1Ko 15:30
2Ko 11:23
Flp 2:29
j 1Th 1:1
1Pe 5:12
k Mdo 16:4
l Yoh 16:13
Mdo 5:32
m Mt 23:4
n Mwa 35:2
Kut 20:3
Kut 34:15
Eze 20:30
1Ko 8:1
1Ko 10:14
o Mwa 9:4
Law 3:17
Law 7:26
Law 17:10
Kum 12:16
Kum 12:23
1Sa 14:32
p Law 17:13
q Mwa 39:9
1Ko 6:9
Efe 5:5
Kol 3:5
1Th 4:3
1Pe 4:3
r Mdo 21:25

naomhubiri, kwa sababu yeye
husomwa kwa sauti kubwa ka-
tika masinagogi kila siku ya
sabato."[a]

22 Ndipo mitume na wanau-
me wazee pamoja na kutaniko
lote wakapendelea kutuma wa-
naume waliochaguliwa kutoka
kati yao mpaka Antiokia pamo-
ja na Paulo na Barnaba, yaa-
ni, Yuda aliyeitwa Barsaba[b] na
Sila, wanaume wenye kuongo-
za kati ya akina ndugu; **23** na
kwa mkono wao wakaandika:

"Mitume na wanaume wazee,
akina ndugu, kwa wale ndu-
gu katika Antiokia[c] na Si-
ria na Kilikia[d] ambao ni wa
kutoka kwa mataifa: Salamu!
24 Kwa kuwa tumesikia kwa-
mba baadhi ya wale waliotoka
kati yetu wamewataabisha ni-
nyi kwa maneno mengi,[e] wa-
kijaribu kupindua nafsi zenu,
ijapokuwa sisi hatukuwapa
maagizo yoyote,[f] **25** sisi tu-
mefikia kauli moja[g] nasi tu-
mependelea kuchagua wana-
ume tuwatume kwenu pamo-
ja na wapendwa wetu, Barna-
ba na Paulo,[h] **26** watu ambao
wametoa nafsi zao kwa ajili ya
jina la Bwana wetu Yesu Kri-
sto.[i] **27** Kwa hiyo tunawatu-
ma Yuda na Sila,[j] ili wao pia wa-
pate kueleza mambo hayohayo
kwa maneno.[k] **28** Kwa maa-
na roho takatifu[l] na sisi wenye-
we tumependelea tusiwaonge-
zee ninyi mzigo[m] zaidi, ila ma-
mbo haya ya lazima, **29** kue-
ndelea kujiepusha na vitu
vilivyotolewa dhabihu kwa sa-
namu[n] na damu[o] na vitu vili-
vyonyongwa[p] na uasherati.[q]
Mkijiepusha kwa uangalifu na
mambo haya,[r] mtafanikiwa.
Afya njema kwenu!"

30 Basi, watu hawa wa-
lipoachwa waende, wakashu-
ka kwenda Antiokia, nao wa-
kaukusanya umati pamoja na
kuwapa barua hiyo.[a] **31** Ba-
ada ya kuisoma, walishangi-
lia juu ya kitia-moyo hicho.[b]
32 Nao Yuda na Sila, kwa kuwa
wao wenyewe walikuwa mana-
bii[c] pia, wakawatia moyo aki-
na ndugu kwa hotuba nyingi
na kuwatia nguvu.[d] **33** Kwa
hiyo, baada ya kukaa huko kwa
muda fulani, ndugu hao wa-
kawaacha waende kwa amani[e]
kwa wale waliokuwa wamewa-
tuma. **34** —— **35** Hata hi-
vyo, Paulo na Barnaba waka-
endelea kukaa Antiokia[f] waki-
fundisha na kutangaza habari
njema ya neno la Yehova, wa-
kiwa pamoja na wengine wengi
pia.[g]
36 Sasa baada ya siku ka-
dhaa Paulo akamwambia Ba-
rnaba: "Zaidi ya mambo yote,
na turudi tuwatembelee akina
ndugu katika kila moja la ma-
jiji ambamo tulitangaza neno
la Yehova tuone jinsi walivyo."[h]
37 Barnaba alikuwa ameazi-
mia kumchukua Yohana pia,
aliyeitwa Marko.[i] **38** Lakini
Paulo hakuona kwamba inafaa
kumchukua huyo pamoja nao,
kwa kuwa alikuwa amewaa-
cha kule Pamfilia[j] na hakuwa
ameenda pamoja nao kwenye
kazi. **39** Ndipo kukatokea
hasira kali, hivi kwamba waka-
tengana; Barnaba[k] akamchu-
kua Marko pamoja naye na ku-
safiri kwenda Kipro.[l] **40** Pau-
lo akamchagua Sila[m] akaondo-
ka kwenda zake baada ya kuwa
amekabidhiwa na akina ndugu
kwenye fadhili zisizostahiliwa
za Yehova.[n] **41** Lakini akapi-
tia Siria na Kilikia, akiyatia
nguvu makutaniko.[a]

16 Kwa hiyo akafika Derbe
na pia Listra.[b] Na, tazama!
mwanafunzi fulani aliye-
itwa Timotheo[c] alikuwa huko,
mwana wa mwanamke Mya-
hudi aliye mwamini lakini wa
baba Mgiriki, **2** naye alishu-
hudiwa vema na akina ndu-
gu katika Listra na Ikoniamu.
3 Paulo alitamani mtu huyu
aende pamoja naye, naye aka-
mchukua na kumtahiri[d] kwa
sababu ya Wayahudi waliooku-
wa katika sehemu hizo, kwa
maana wote walijua kwamba
baba yake ni Mgiriki. **4** Basi
walipoendelea kusafiri kupitia
katika majiji walikuwa waki-
wapa wale waliokuwa huko
maagizo yaliyokuwa yameamu-
liwa na mitume na wanaume
wazee waliokuwa katika Yeru-
salemu ili wayashike.[e] **5** Kwa
hiyo, kwa kweli, makutaniko
yakaendelea kufanywa imara
katika imani[f] na kuongezeka
hesabu siku baada ya siku.
6 Zaidi ya hayo, wakapitia
Frigia na nchi ya Galatia,[g] kwa
sababu walikatazwa na roho ta-
katifu wasiseme lile neno katika
wilaya ya Asia. **7** Tena,
walipofika Misia wakafanya jiti-
hada za kuingia Bithinia,[h] laki-
ni roho ya Yesu haikuwaruhusu.
8 Kwa hiyo wakapita Mi-
sia na kushuka mpaka Troa.[i]
9 Na usiku maono[j] yakamto-
kea Paulo: mwanamume fula-
ni Mmakedonia alikuwa amesi-
mama akimsihi na kusema:
"Vuka uingie Makedonia utusa-
idie." **10** Basi mara tu alipo-
kuwa amekwisha kuona maono
hayo, tukajaribu kuingia Make-
donia,[k] tukikata kauli kwamba

SURA 15
a Mdo 11:26
b Met 15:30
c Mdo 11:27
Mdo 13:1
d Mdo 13:15
Mdo 18:23
e 1Ko 16:11
f Mdo 13:1
g 2Ko 11:7
h 2Ko 11:28
i Kol 4:10
2Ti 4:11
j Mdo 13:13
k Mdo 4:36
Mdo 13:4
l Mdo 11:20
m Mdo 15:27
n Mdo 14:26
Efe 3:7

Safu ya 2
a Mdo 16:5

SURA 16
b Mdo 14:6
2Ti 3:11
c Mdo 19:22
Ro 16:21
1Ko 4:17
1Th 3:2
1Ti 1:2
d 1Ko 9:20
e Mdo 15:28
f Mdo 15:41
g Mdo 18:23
Ga 4:13
h 1Pe 1:1
i 2Ko 2:12
2Ti 4:13
j Ayu 33:15
Mdo 9:10
2Ko 12:1
k 2Ko 1:16
2Ko 2:13

Mungu alikuwa ametuita tuwatangazie habari njema.

11 Kwa hiyo tukasafiri baharini kutoka Troa na kuja kwa safari ya moja kwa moja mpaka Samothrake, lakini siku iliyofuata tukaja mpaka Neapoli, **12** na kutoka huko mpaka Filipi,[a] koloni, ambalo ni jiji kuu la wilaya ya Makedonia.[b] Tukakaa katika jiji hili kwa siku kadhaa. **13** Na siku ya sabato tukatoka nje ya lango kando ya mto, ambapo tulikuwa tukifikiri kwamba palikuwa na mahali pa sala; nasi tukaketi na kuanza kusema na wanawake waliokuwa wamekusanyika. **14** Na mwanamke fulani anayeitwa Lidia, muuzaji wa nguo za rangi ya zambarau, wa jiji la Thiatira[c] aliyekuwa mwabudu wa Mungu, alikuwa akisikiliza, na Yehova akafungua wazi moyo[d] wake asikilize kwa makini mambo yaliyokuwa yakisemwa na Paulo. **15** Basi yeye na watu wa nyumbani mwake walipobatizwa,[e] akasema hivi kwa kusihi: "Ikiwa ninyi mmeniona kuwa mwaminifu kwa Yehova, ingieni ndani ya nyumba yangu mkae."[f] Naye akatushurutisha kwelikweli.[g]

16 Na ikatukia kwamba tulipokuwa tukienda pale mahali pa sala, kijakazi fulani mwenye roho,[h] roho mwovu wa uaguzi,[i] akakutana nasi. Yeye alikuwa akiwapatia mabwana zake faida[j] nyingi kwa kufanya ufundi wa kubashiri. **17** Kijakazi huyo alikuwa akimfuata Paulo na sisi akipaaza sauti[k] kwa maneno haya: "Watu hawa ni watumwa wa Mungu Aliye Juu Zaidi, wanaowatangazia ninyi njia ya wokovu." **18** Akaendelea kufanya hivyo kwa siku nyingi. Mwishowe Paulo akachoshwa,[a] akageuka na kumwambia huyo roho: "Ninakuagiza katika jina la Yesu Kristo umtoke."[b] Naye akatoka saa hiyohiyo.[c]

19 Basi, mabwana zake walipoona kwamba tumaini lao la kupata faida lilikuwa limeondoka,[d] wakamshika Paulo na Sila wakawakokota na kuwapeleka sokoni kwa watawala,[e] **20** wakawapeleka mpaka kwa mahakimu wa raia, wakasema: "Watu hawa wanasumbua[f] sana jiji letu, wao wakiwa ni Wayahudi, **21** nao wanatangaza desturi[g] ambazo si halali kwetu kuzikubali au kuzitenda, kwa kuwa sisi ni Waroma." **22** Nao umati ukasimama pamoja dhidi yao; na wale mahakimu wa raia, baada ya kuyararua mavazi yao ya nje, wakatoa amri wapigwe kwa fimbo.[h] **23** Baada ya kuwapiga mapigo mengi,[i] wakawatupa gerezani, wakimwagiza mlinzi wa jela awalinde.[j] **24** Kwa sababu alipata agizo la namna hiyo, akawatupa ndani ya gereza[k] la ndani zaidi na kuifunga miguu yao katika mikatale.[l]

25 Lakini karibu na katikati ya usiku[m] Paulo na Sila walikuwa wakisali na kumsifu Mungu kwa wimbo;[n] ndiyo, wafungwa walikuwa wakiwasikia. **26** Kwa ghafula tetemeko kubwa la nchi likatukia, hivi kwamba misingi ya jela ikatikiswa. Zaidi ya hayo, milango yote ikafunguka mara moja, na vifungo vya wote vikafunguka.[o] **27** Mlinzi wa jela, alipoamka kutoka usingizini na kuona milango ya gereza

SURA 16

a Flp 1:1
1Th 2:2
b Mdo 20:6
c Ufu 1:11
d Lu 24:45
1Ko 3:7
e Mdo 16:33
Mdo 18:8
f Mt 10:11
Ro 12:13
Ga 6:6
Ebr 13:2
g Mwa 19:2
Amu 19:20
Lu 24:29
h 1Sa 28:7
i Law 19:31
Law 20:6
j Mdo 19:24
k Mk 1:24
Lu 4:41

Safu ya 2

a Mk 1:25
b Mk 1:34
Lu 9:1
Lu 10:17
c Mt 17:18
d Mdo 19:25
e Mt 10:18
2Ko 6:5
f 1Fa 18:17
Mdo 17:6
g Est 3:8
h 1Th 2:2
i 2Ko 11:23
j Lu 21:12
Mdo 5:23
k Mdo 12:6
Mdo 12:10
l Zb 105:18
Yer 20:2
m Zb 42:8
n Efe 5:19
Kol 3:16
Yak 5:13
o Mdo 4:31
Mdo 5:19
Mdo 12:7

ilikuwa imefunguka, akauchomoa upanga wake na alikuwa karibu kujiua,[a] akiwazia kwamba wafungwa walikuwa wametoroka.[b] **28** Lakini Paulo akapaaza sauti kubwa, akisema: "Usijiumize,[c] kwa maana sisi sote tupo hapa!" **29** Kwa hiyo akaomba taa akaruka ndani na, akitetemeka, akaanguka chini[d] mbele ya Paulo na Sila. **30** Naye akawaleta nje na kusema: "Mabwana zangu, nifanye[e] nini ili niokolewe?" **31** Wakasema: "Mwamini Bwana Yesu nawe utaokolewa,[f] wewe na watu wa nyumba yako."[g] **32** Nao wakamwambia neno la Yehova pamoja na wale wote walio katika nyumba yake.[h] **33** Naye akawachukua pamoja naye katika saa hiyo ya usiku akaosha mapigo yao; na, wote, yeye na walio wake wakabatizwa[i] bila kukawia. **34** Naye akawaleta ndani ya nyumba yake na kutandika meza mbele yao, naye akashangilia sana pamoja na watu wote wa nyumba yake kwa kuwa sasa alikuwa amemwamini Mungu.

35 Ilipokuwa mchana mahakimu wa raia[j] wakawatuma maofisa wa polisi wakaseme: "Wafungue wale watu." **36** Kwa hiyo mlinzi wa jela akamweleza Paulo maneno yao: "Mahakimu wa raia wamewatuma watu kwamba ninyi wawili mfunguliwe. Kwa hiyo, sasa, tokeni mwende zenu kwa amani." **37** Lakini Paulo akawaambia: "Walitupiga viboko hadharani bila kuhukumiwa kuwa wenye hatia, sisi tulio Waroma,[k] na kututupa gerezani; na je, sasa wanatufukuza kwa siri? Hapana, hata kidogo! lakini acha wao wenyewe waje watutoe nje." **38** Kwa hiyo wale maofisa wa polisi wakawaeleza mahakimu wa raia maneno hayo. Nao wakaogopa waliposikia kwamba watu hao walikuwa Waroma.[a] **39** Kwa hiyo wakaja na kuwasihi na, baada ya kuwatoa nje, wakawaomba waondoke katika jiji hilo. **40** Lakini wakatoka katika gereza hilo na kwenda nyumbani kwa Lidia, nao walipowaona akina ndugu wakawatia moyo,[b] wakaondoka.

17 Sasa wakasafiri kupitia Amfipoli na Apolonia wakaja mpaka Thesalonike,[c] ambako kulikuwa na sinagogi la Wayahudi. **2** Basi kulingana na desturi ya Paulo[d] akaingia ndani walimokuwa, na kwa sabato tatu akajadiliana nao kwa kutumia Maandiko,[e] **3** akieleza na kuthibitisha kwa marejeo kwamba ilikuwa lazima Kristo ateseke[f] na kufufuliwa kutoka kwa wafu,[g] akisema: "Huyu ndiye Kristo,[h] Yesu huyu ninayewatangazia ninyi." **4** Ikawa kwamba baadhi yao wakawa waamini[i] na kujiunga na Paulo na Sila,[j] na umati mkubwa kati ya Wagiriki waliomwabudu Mungu na si wachache kati ya wanawake wenye vyeo waliofanya hivyo.

5 Lakini Wayahudi wakawa na wivu,[k] wakashirikiana na wanaume fulani waovu kati ya wazururaji wa sokoni na kufanyiza kikundi chenye ghasia ili kuzusha fujo jijini.[l] Nao wakaishambulia nyumba ya Yasoni[m] na kuanza kujaribu kuwaleta mbele ya watu wenye kufanya ghasia. **6** Wali-

SURA 16
a Mdo 12:19
b 1Fa 20:39
c 1Th 5:15
d Mdo 10:25
e Mdo 2:37
f Yoh 3:16
Yoh 6:47
g Mdo 11:14
h Mdo 10:24
i Mdo 8:12
Mdo 16:15
j Mdo 16:20
k Mdo 22:25
Mdo 23:27

Safu ya 2
a Mdo 22:29
b Lu 22:32
2Ko 1:4

SURA 17
c 1Th 2:1
d Mdo 9:20
Mdo 13:14
Mdo 14:1
Mdo 18:4
e Mdo 18:19
f Zb 22:7
Zb 22:16
Zb 34:20
Zb 69:21
Zb 118:22
Isa 50:6
Isa 53:3
Isa 53:5
g Zb 16:10
Lu 24:46
h Mdo 18:28
Ga 3:1
i Mdo 28:24
j Mdo 15:22
Mdo 15:40
k Mdo 13:45
l Mdo 16:20
m Ro 16:21

powakosa wakamkokota Yasoni na akina ndugu fulani na kuwapeleka kwa watawala wa jiji, wakipaaza sauti hivi: "Watu hawa ambao wameipindua[a] dunia inayokaliwa wapo hapa pia, **7** na Yasoni amewakaribisha. Na watu wote hawa wanapingana na maagizo[b] ya Kaisari, wakisema kuna mfalme[c] mwingine, Yesu." **8** Kwa kweli walifadhaisha huo umati na watawala wa jiji waliposikia mambo haya; **9** na kwanza baada ya kuchukua dhamana ya kutosha kutoka kwa Yasoni na wale wengine wakawaacha waende zao.

10 Mara moja wakati wa usiku[d] akina ndugu wakatuma Paulo na Sila pia mpaka Beroya, na hawa, walipofika, wakaingia katika sinagogi la Wayahudi. **11** Sasa watu hawa walikuwa wasikivu kuliko wale wa Thesalonike, kwa maana walilipokea neno kwa hamu kubwa zaidi ya akili, wakiyachunguza[e] Maandiko[f] kwa uangalifu kila siku ili kuona kama mambo hayo ndivyo yalivyo.[g] **12** Kwa hiyo wengi kati yao wakawa waamini, na pia walioamini kati ya wanawake Wagiriki wenye kusifika[h] na kati ya wanaume si wachache. **13** Lakini Wayahudi kutoka Thesalonike walipopata habari kwamba Paulo alitangaza neno la Mungu katika Beroya pia, wakaja huko pia ili kuchochea[i] na kuwafadhaisha[j] watu. **14** Ndipo akina ndugu wakamsindikiza Paulo mara moja mpaka baharini;[k] lakini Sila na Timotheo pia wakabaki nyuma huko. **15** Hata hivyo, wale waliokuwa wakimsindikiza Paulo wakamleta mpaka Athene na, baada ya kupokea amri kwamba Sila na Timotheo[a] wamfuate upesi iwezekanavyo, wakaondoka.

16 Basi Paulo alipokuwa akiwangojea katika Athene, roho yake ikaudhika[b] ndani yake alipoona kwamba jiji hilo lilikuwa limejaa sanamu. **17** Kwa hiyo akaanza kujadiliana katika sinagogi pamoja na Wayahudi[c] na watu wengine waliomwabudu Mungu na kila siku sokoni[d] pamoja na wale waliokuwapo. **18** Lakini watu fulani kati ya Waepikurea na wanafalsafa[e] Wastoa pia wakawa wanaongea naye kwa mabishano, na baadhi yao walikuwa wakisema: "Mpiga-domo huyu angependa kueleza jambo gani?"[f] Wengine: "Anaonekana kuwa mtangazaji wa miungu migeni." Kwa sababu alikuwa akitangaza habari njema ya Yesu na ufufuo.[g] **19** Kwa hiyo wakamshika na kumpeleka Areopago, wakisema: "Je, tunaweza kujua ni fundisho gani hili jipya[h] unalosema? **20** Kwa maana unaanzisha mambo yaliyo mageni masikioni mwetu. Kwa hiyo tunataka kujua mambo haya yanamaanisha nini."[i] **21** Kwa kweli, Waathene wote na wageni waliokuwa wakikaa huko kwa muda hawakuwa wakitumia wakati wao wa starehe wakifanya chochote ila kuambiana jambo au kusikiliza jambo jipya. **22** Basi Paulo akasimama katikati ya Areopago[j] na kusema:

"Wanaume wa Athene, ninaona kwamba katika mambo yote mnaonekana kuwa wenye mwelekeo zaidi wa kuogopa miungu[k]

SURA 17

a 1Fa 18:17
Mdo 16:20

b Ezr 4:12

c Lu 23:2
Yoh 19:12

d Mdo 9:25

e Lu 16:29

f Yoh 5:39

g Met 14:15

h Mdo 13:50

i Mdo 14:19
1Th 2:15

j Mdo 14:2

k Mt 10:23

Safu ya 2

a Mdo 16:1
1Th 3:2

b 2Pe 2:8

c Mdo 13:5
Mdo 18:19

d Met 1:20

e 1Ko 1:22
Kol 2:8

f 1Ko 4:13

g Yoh 5:29
Yoh 11:25
1Ko 15:12
Ufu 20:6

h Mk 1:27

i Mdo 2:12

j Mdo 17:34

k Mdo 17:16

kuliko wengine. **23** Kwa mfano, nilipokuwa nikipita njiani
na kutazama kwa uangalifu
vitu vyenu vya ibada, niliona
pia madhabahu ambayo ilikuwa imeandikwa 'Kwa Mungu
Asiyejulikana.' Kwa hiyo kile
mnachokipa ujitoaji-kimungu
bila kujua, hicho ninawatangazia ninyi. **24** Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote
vilivyomo, akiwa, kama Huyu
alivyo, Bwana wa mbingu na
dunia,[a] hakai katika mahekalu yaliyofanywa kwa mikono,[b]
25 wala hatumikiwi kwa mikono ya binadamu kana kwamba anahitaji kitu chochote,[c]
kwa sababu yeye mwenyewe
huwapa watu wote uhai[d] na pumzi[e] na vitu vyote. **26** Naye
alifanya kutoka kwa mtu mmoja[f] kila taifa[g] la watu, ili wakae juu ya uso wa dunia nzima,[h] naye aliamuru nyakati[i]
na mipaka ya makao ya watu,[j]
27 ili wao wamtafute Mungu,[k]
ikiwa wangeweza kupapasapapasa wakimtafuta na kwa
kweli wampate,[l] ijapokuwa,
kweli, hayuko mbali sana na
kila mmoja wetu. **28** Kwa
maana kupitia kwake tuna
uhai na tunaenda na kuwako,[m]
hata kama vile ambavyo watu
fulani ambao ni washairi[n] kati
yenu wamesema, 'Kwa maana
sisi pia ni uzao wake.'

29 "Kwa hiyo, kwa kuwa sisi
ni uzao wa Mungu,[o] hatupaswi kuwazia kwamba Mungu[p]
ni kama dhahabu au fedha au
jiwe, kama kitu kilichochongwa
kwa ufundi na mtungo wa mwanadamu.[q] **30** Ni kweli, Mungu
ameachilia mbali nyakati hizo
za kutojua,[r] lakini sasa anawaambia wanadamu wote kila ma-

SURA 17

a Zb 146:6
Isa 42:5
Mdo 4:24
Mdo 14:15
b 1Fa 8:27
Isa 66:1
Mdo 7:48
c Zb 50:12
d Mwa 2:7
e Isa 42:5
f Mwa 5:2
g Mwa 1:28
h Kum 32:8
i Zb 74:17
j Kum 2:5
Kum 2:19
Kum 32:8
Isa 34:17
k Kum 4:29
Isa 55:6
l Zb 145:18
Yer 23:23
Ro 1:20
m Isa 42:5
n Tit 1:12
o Mwa 1:27
p Yos 22:22
Zb 50:1
Isa 46:9
q Kum 5:8
Isa 37:19
Isa 40:18
Isa 46:5
Mdo 19:26
r Mdo 14:16
Ro 3:25
Ro 5:13
Efe 4:18

Safu ya 2

a Lu 24:47
b Zb 96:13
Zb 98:9
Isa 2:4
Yoh 5:22
Mdo 10:42
c Yoh 11:25
Mdo 2:24
Mdo 13:33
Ro 6:5
d 1Ko 1:23
e Mdo 17:19

SURA 18

f Mdo 18:26
1Ko 16:19
2Ti 4:19
g Ebr 13:24
h Mdo 11:28
i Mdo 20:34
1Ko 4:12
1Ko 9:15
1Th 2:9
2Th 3:10
j Mt 4:23
Mdo 13:14
Mdo 17:2
k Mdo 15:27
Mdo 17:14
l Mdo 16:1
1Th 3:6

hali kwamba wanapaswa kutubu.[a] **31** Kwa sababu ameweka
siku ambayo katika hiyo anakusudia kuihukumu[b] kwa uadilifu
dunia inayokaliwa kupitia kwa
mwanamume ambaye amemweka rasmi, naye ametoa uhakikisho kamili kwa watu wote kwa
kuwa amemfufua[c] kutoka kwa
wafu."

32 Basi, waliposikia juu ya
ufufuo wa wafu, wengine kati
yao wakaanza kudhihaki,[d] huku
wengine wakisema: "Tutakusikiliza tena juu ya jambo hili
wakati mwingine." **33** Hivyo
Paulo akatoka katikati yao,
34 lakini wanaume fulani wakajiunga naye na kuwa waamini, kati yao pia wakiwa ni Dionisio, mwamuzi wa mahakama ya Areopago,[e] na mwanamke mmoja aliyeitwa Damari,
na wengine mbali na hao.

18 Baada ya hayo akaondoka Athene na kuja Korintho. **2** Naye akamkuta Myahudi fulani anayeitwa Akila,[f]
mzaliwa wa Ponto ambaye alikuwa amekuja hivi karibuni
kutoka Italia,[g] na Prisila mke
wake, kwa sababu Klaudio[h]
alikuwa ameagiza Wayahudi
wote waondoke Roma. Kwa
hiyo akawaendea **3** na kwa
sababu ya kuwa wa kazi ileile akakaa nyumbani kwao, nao
wakafanya kazi,[i] kwa maana
kazi yao ilikuwa ya kutengeneza mahema. **4** Hata hivyo,
yeye alikuwa akitoa hotuba
katika sinagogi[j] kila sabato
na alikuwa akiwashawishi Wayahudi na Wagiriki.

5 Basi, Sila[k] na Timotheo[l]
pia waliposhuka kutoka Makedonia, Paulo akaanza kushu-

ghulika sana na lile neno, akiwatolea Wayahudi ushahidi ili
kuthibitisha kwamba Yesu ndiye Kristo.[a] **6** Lakini walipoendelea kupinga na kutukana,[b]
akayakung'uta mavazi[c] yake
na kuwaambia: "Damu[d] yenu
na iwe juu ya vichwa vyenu
wenyewe. Mimi ni safi.[e] Tangu sasa na kuendelea nitaenda kwa watu wa mataifa."[f]
7 Basi akahama huko na kuingia katika nyumba ya mwanamume anayeitwa Titio Yusto,
mwabudu wa Mungu, ambaye
nyumba yake ilikuwa inashikana na sinagogi. **8** Lakini Krispo[g] ofisa-msimamizi wa sinagogi akawa mwamini katika
Bwana, na ndivyo na watu wote
wa nyumba yake. Na wengi kati
ya Wakorintho waliosikia wakaanza kuamini na kubatizwa.
9 Zaidi ya hayo, wakati wa usiku Bwana akamwambia Paulo[h]
kupitia maono: "Usiogope, bali
endelea kusema wala usinyamaze, **10** kwa sababu mimi
nipo pamoja na wewe[i] na hakuna mtu atakayekushambulia
ili kukutendea jambo baya; kwa
maana nina watu wengi katika jiji hili." **11** Kwa hiyo akakaa huko bila kuondoka kwa
mwaka mmoja na miezi sita,
akifundisha kati yao neno la
Mungu.

12 Sasa Galio alipokuwa liwali[j] wa Akaya, Wayahudi wa-
kasimama kwa umoja dhidi ya
Paulo na kumwongoza kwenye
kiti cha hukumu,[k] **13** wakisema: "Mtu huyu huongoza
watu kinyume cha sheria[l] kwe-
nye sadikisho lingine katika
kumwabudu Mungu." **14** Lakini Paulo alipokuwa akitaka
kufungua kinywa chake, Galio

SURA 18

a Mdo 17:3
Mdo 28:23

b 1Pe 4:4

c Mt 10:14
Mdo 13:51

d 1Fa 2:37
Eze 18:13
Eze 33:4

e Eze 3:18
Mdo 20:26

f Mdo 13:46
Mdo 28:28
Ro 1:16

g 1Ko 1:14

h Lu 22:43
Mdo 23:11

i Yer 1:19
Mt 28:20

j Mdo 13:7
Mdo 19:38

k Mdo 16:19

l Mdo 24:5

Safu ya 2

a 1Ti 6:4

b Mdo 23:29
Mdo 25:19

c 1Ko 1:1

d Hes 6:18
Mdo 21:23

e Ro 16:1

f Mdo 13:14
Mdo 17:2

g Mdo 21:6

h Ro 1:10
1Ko 4:19
Yak 4:15

akawaambia Wayahudi: "Kama
kwa kweli lingekuwa ni kosa
fulani au tendo baya la uhalifu, enyi Wayahudi, ningekuwa
na sababu ya kuwavumilia ninyi. **15** Lakini kama ni mabishano juu ya maneno na majina[a] na sheria[b] kati yenu, amu-
eni ninyi wenyewe. Mimi sitaki kuwa mwamuzi wa mambo
haya." **16** Ndipo akawafukuza kutoka mbele ya kiti cha hu-
kumu. **17** Kwa hiyo wote wakamshika Sosthene[c] ofisa-msi-
mamizi wa sinagogi na kuanza
kumpiga mbele ya kiti cha hukumu. Lakini Galio hakujiha-
ngaisha hata kidogo na mambo
hayo.

18 Hata hivyo, baada ya kukaa siku kadhaa zaidi, Paulo aliwaaga akina ndugu naye
akaendelea kusafiri kwenda Siria, na pamoja naye Prisila
na Akila, kwa kuwa nywele
za kichwa chake zilikuwa zimekatwa[d] katika Kenkrea,[e] kwa
maana alikuwa ameweka na-
dhiri. **19** Kwa hiyo wakafika
Efeso, naye akawaacha huko;
lakini yeye mwenyewe akaingia ndani ya sinagogi[f] akaja-
diliana na Wayahudi. **20** Ija-
pokuwa waliendelea kumwomba akae kwa muda mrefu
zaidi, hakukubali **21** bali aka-
waaga[g] na kuwaambia: "Nita-
rudi kwenu tena, ikiwa Yeho-
va anapenda."[h] Naye akasafiri
baharini kutoka Efeso **22** na
kushuka mpaka Kaisaria. Naye
akapanda kwenda, akalisalimu
kutaniko, na kushuka kwenda
Antiokia.

23 Na alipokuwa amekaa huko kwa wakati fulani akaon-
doka na kwenda kutoka ma-
hali mpaka mahali kupitia nchi

ya Galatia[a] na Frigia,[b] akiwatia
nguvu[c] wanafunzi wote.
24 Sasa Myahudi fulani anayeitwa Apolo,[d] mzaliwa wa Aleksandria, mwanamume mfasaha, akafika Efeso; naye alikuwa mwenye ujuzi mwingi sana wa Maandiko.[e] **25** Mwanamume huyu alikuwa amefundishwa njia ya Yehova kwa mdomo, kwa kuwa alikuwa amewaka roho,[f] akaanza kusema na kuyafundisha kwa usahihi mambo juu ya Yesu, lakini akiwa anaufahamu ubatizo[g] wa Yohana tu. **26** Na mwanamume huyo akaanza kusema kwa ujasiri katika sinagogi. Prisila na Akila[h] walipomsikia, wakamchukua na kumfafanulia kwa usahihi zaidi njia ya Mungu. **27** Tena, kwa sababu alikuwa akitaka kuvuka aingie Akaya, akina ndugu wakawaandikia wanafunzi, wakiwahimiza wamkaribishe kwa fadhili. Kwa hiyo alipofika huko, akawasaidia[i] sana wale waliokuwa wameamini kwa sababu ya fadhili zisizostahiliwa[j] za Mungu; **28** kwa maana kwa juhudi nyingi alithibitisha kikamili hadharani kuwa Wayahudi ni wenye makosa, huku akionyesha kwa Maandiko[k] kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo.[l]

19 Ikawa, Apolo[m] alipokuwa Korintho, Paulo akapita barani na kushuka mpaka Efeso,[n] akakuta wanafunzi fulani; **2** akawaambia: "Je, mlipokea roho takatifu[o] mlipokuwa waamini?" Wakamwambia: "Lo! hatujapata kusikia kamwe kama kuna roho takatifu."[p] **3** Naye akasema: "Basi, mlibatizwa katika nini?" Wakasema: "Katika ubatizo wa Yohana."[q]

SURA 18

a Ga 1:2
b Mdo 16:6
c Mdo 14:22
Mdo 15:32
d Mdo 19:1
1Ko 1:12
1Ko 3:6
e 1Ko 4:6
f Ro 12:11
g Mdo 19:3
h Ro 16:3
1Ko 16:19
i 1Ko 3:6
j Efe 2:8
k Lu 24:27
1Ko 15:3
2Ti 3:16
l Mwa 49:10
Kum 18:15
Zb 16:10
Isa 7:14
Mik 5:2
Mal 3:1
Mdo 9:22

SURA 19

m Mdo 18:24
1Ko 3:5
n 1Ko 16:8
o Mdo 2:38
p Mdo 8:16
q Mdo 18:25

Safu ya 2

a Mt 3:11
Mk 1:4
Mdo 1:5
b Yoh 1:15
Yoh 1:30
c Mdo 8:16
d Mdo 8:17
e Mdo 2:4
Mdo 10:46
1Ko 12:10
f Lu 4:16
Mdo 13:5
Mdo 17:2
g Mdo 1:3
Mdo 28:23
Mdo 28:31
h 2Th 3:2
i Mdo 9:2
Mdo 22:4
j Mt 10:14
Ro 16:17
k Tit 3:10
2Yo 10
l Mdo 20:31
m Mdo 20:18
2Ti 1:15
n Mdo 14:3
o Mk 6:56
Mdo 5:15
p Mt 10:1
q Mt 12:27
r Mk 9:38
Lu 9:49

4 Paulo akasema: "Yohana alibatiza kwa ubatizo unaoonyesha toba,[a] akiwaambia watu wamwamini yule ambaye angekuja baada yake,[b] yaani, Yesu." **5** Waliposikia hilo, wakabatizwa katika jina la Bwana Yesu.[c] **6** Na Paulo alipoweka mikono[d] yake juu yao, roho takatifu ikaja juu yao, nao wakaanza kusema katika lugha na kutoa unabii.[e] **7** Wote pamoja walikuwa wanaume karibu kumi na wawili.

8 Akaingia katika sinagogi,[f] akasema kwa ujasiri kwa miezi mitatu, akitoa hotuba na kutumia ushawishi kuhusu ufalme[g] wa Mungu. **9** Lakini wengine walipoendelea kujifanya wenyewe wagumu na kutoamini,[h] wakisema vibaya juu ya Ile Njia[i] mbele ya umati, akaondoka kwao[j] na kuwatenga wanafunzi kutoka kwao,[k] kila siku akitoa hotuba nyingi katika jumba la shule ya Tirano. **10** Jambo hilo lilitukia kwa muda wa miaka miwili,[l] hivi kwamba wale wote waliokuwa wakikaa katika wilaya ya Asia[m] wakasikia neno la Bwana, Wayahudi na Wagiriki pia.

11 Na Mungu akazidi kufanya kazi za nguvu zinazozidi za kawaida kupitia mikono ya Paulo,[n] **12** hivi kwamba hata nguo na vitambaa vilichukuliwa kutoka katika mwili wake na kupelekwa kwa watu wenye kuugua,[o] na magonjwa yakawaacha, na roho waovu wakatoka.[p] **13** Lakini watu fulani kati ya Wayahudi wenye kuzunguka-zunguka waliozoea kazi ya kufukuza roho waovu[q] pia wakachukua daraka la kuliitia jina la Bwana Yesu[r] juu ya wale

wenye roho waovu, wakisema:
"Mimi ninawaagiza[a] ninyi kwa
uzito kwa Yesu ambaye Pau-
lo humhubiri." **14** Sasa kuli-
kuwa na wana saba wa Ske-
wa, mkuu wa makuhani wa Ki-
yahudi, wakifanya jambo hilo.
15 Lakini roho mwovu akawa-
jibu, akawaambia: "Mimi nina-
mjua Yesu[b] nami ninamfahamu
Paulo;[c] lakini ninyi ni nani?"
16 Ndipo mtu huyo ambaye
huyo roho mwovu alikuwa nda-
ni yake akawarukia,[d] akawa-
zidi nguvu mmoja baada ya
mwingine, na kuwashinda, hivi
kwamba wakakimbia kutoka
nyumba hiyo wakiwa uchi na
wakiwa wameumizwa. **17** Ja-
mbo hilo likajulikana na wote,
Wayahudi na Wagiriki pia wa-
liokaa katika Efeso; na woga[e]
ukawaingia hao wote, na jina la
Bwana Yesu likaendelea kutu-
kuzwa.[f] **18** Na wengi kati ya
wale waliokuwa waamini wa-
kawa wanakuja na kuungama[g]
na kueleza juu ya mazoea yao
waziwazi. **19** Kwa kweli, he-
sabu kubwa ya wale waliozo-
ea kufanya ufundi wa uchawi[h]
wakaleta pamoja vitabu vyao
wakaviteketeza mbele ya kila
mtu. Nao wakapiga pamoja he-
sabu za bei zake na kupata vi-
kiwa na thamani ya vipande
50,000 vya fedha. **20** Hivyo
katika njia yenye nguvu neno
la Yehova likazidi kukua na ku-
sitawi.[i]

21 Sasa mambo hayo yalipo-
kuwa yametimizwa, Paulo aka-
kusudia katika roho yake kwa-
mba, baada ya kupitia Makedo-
nia[j] na Akaya, angefunga safari
kwenda Yerusalemu,[k] akisema:
"Baada ya kufika huko lazi-
ma pia nione Roma."[l] **22** Kwa
hiyo akawatuma wawili kati
ya wale waliomhudumia, Timo-
theo[a] na Erasto,[b] waende Ma-
kedonia lakini yeye mwenyewe
akakawia kwa wakati fulani ka-
tika wilaya ya Asia.

23 Wakati huo kukatokea
mvurugo[c] usio mdogo kuhusu
Ile Njia.[d] **24** Kwa maana mtu
fulani anayeitwa jina Deme-
trio, fundi wa fedha, kwa ku-
fanya vihekalu vya fedha vya
Artemi aliwapa mafundi ma-
pato ya faida[e] isiyo ndogo;
25 naye akawakusanya hao na
wale waliofanya kazi ya kute-
ngeneza vitu vya namna hiyo[f]
na kusema: "Wanaume, ninyi
mnajua vema kwamba sisi tu-
mepata mafanikio yetu kuto-
kana na biashara hii.[g] **26** Pia,
mnaona na kusikia jinsi si kati-
ka Efeso[h] tu, bali pia katika ka-
ribu wilaya yote ya Asia, Paulo
huyu ameshawishi umati mku-
bwa na kuwageuza kwenye ka-
uli nyingine, akisema kwamba
wale waliofanywa kwa mikono[i]
si miungu. **27** Zaidi ya hayo,
kuna hatari si kwamba tu kazi
hii yetu itapata sifa mbaya bali
pia hekalu la Artemi,[j] mungu
mkuu wa kike, litaonwa kuwa
si kitu na hata utukufu wake
ambao wilaya yote ya Asia na
dunia inayokaliwa huuabudu
utashushwa uwe si kitu hivi
karibuni." **28** Waliposikia ja-
mbo hilo na kujawa na hasi-
ra, watu hao wakaanza kupaa-
za sauti, wakisema: "Artemi wa
Waefeso ni mkuu!"

29 Kwa hiyo jiji likajaa mvu-
rugo, na kwa umoja wakati-
mua mbio na kuingia jumba
la maonyesho, wakawachukua
kwa nguvu pamoja nao Gayo
na Aristarko,[k] Wamakedonia,

SURA 19

a Mdo 16:18

b Mt 8:29
Mk 1:24
Lu 4:34

c Mdo 16:17

d Mt 8:28

e Mdo 2:43
Mdo 5:5

f 2Th 1:12

g Mt 3:6
Yak 5:16

h Kum 18:10
Da 2:2
Mdo 8:9

i Mdo 6:7
Mdo 12:24
Kol 1:6

j 1Ko 16:5

k Mdo 20:22
Ro 15:25

l Mdo 23:11
Ro 1:15

Safu ya 2

a Mdo 16:1

b 2Ti 4:20

c 2Ko 1:8

d Mdo 9:2
Mdo 19:9
Mdo 22:4

e Mdo 16:16

f Zb 115:4

g Ufu 18:15

h Efe 1:1

i Kum 4:28
1Nya 16:26
Isa 44:10
Yer 10:3
Mdo 17:29
1Ko 8:4

j Mdo 19:34

k Mdo 20:4
Kol 4:10
Flm 24

wasafiri waliokuwa wakiandamana na Paulo. **30** Naye Paulo alitaka kuingia walimokuwa watu, lakini wanafunzi hawakumruhusu. **31** Hata baadhi ya wakuu wa sherehe na michezo, waliokuwa wakimwonyesha urafiki, wakatuma watu kwake na kuanza kumwomba asijihatarishe katika mahali pa michezo. **32** Kwa kweli, wengine walikuwa wakipaaza sauti wakisema jambo moja na wengine wakisema lingine;[a] kwa maana kusanyiko lilikuwa katika mvurugo, na walio wengi kati yao hawakujua kwa nini walikuwa wamekusanyika. **33** Kwa hiyo wakiwa pamoja wakamtoa Aleksanda katikati ya umati, Wayahudi wakimsukuma mbele kwa nguvu; na Aleksanda akapunga mkono naye alikuwa akitaka kujitetea mbele ya watu. **34** Lakini walipotambua kwamba alikuwa Myahudi, wote wakapaaza sauti moja kwa karibu saa mbili wakisema: "Artemi wa Waefeso ni mkuu!"[b]

35 Mwishowe, karani wa jiji alipokuwa ameunyamazisha[c] umati, akasema: "Watu wa Efeso, kwa kweli ni nani kati ya wanadamu ambaye hajui kwamba jiji la Efeso ndilo mtunzahekalu wa Artemi mkuu na wa sanamu iliyoanguka kutoka mbinguni? **36** Kwa hiyo, kwa kuwa mambo haya hayawezi kukanushwa, inafaa mtulie na msitende haraka.[d] **37** Kwa maana mmewaleta watu hawa ambao hawaibi katika mahekalu wala hawamkufuru mungu wetu wa kike. **38** Kwa hiyo ikiwa Demetrio[e] na mafundi walio pamoja naye wana kesi juu ya mtu fulani, siku za mahakama[a] hufanywa na kuna maliwali;[b] acheni walete mashtaka mtu juu ya mwenzake. **39** Lakini, ikiwa mnatafuta jambo lolote zaidi ya hilo, lazima liamuliwe katika kusanyiko la kawaida. **40** Kwa maana kwa kweli tunakabili hatari ya kushtakiwa uchochezi wa uasi kuhusu tukio la leo, kukiwa hakuna msingi wowote mmoja tulio nao utakaoturuhusu tutoe sababu ya kikundi hiki chenye machafuko." **41** Na alipokuwa amesema mambo hayo,[c] akaliagiza kusanyiko liende.[d]

20 Sasa baada ya ghasia hizo kutulia, Paulo akatuma watu wawaite wanafunzi, na alipokuwa amewatia moyo na kuwaaga,[e] akasafiri na kuingia Makedonia.[f] **2** Baada ya kupitia sehemu hizo na kuwatia moyo wale walio huko kwa maneno mengi,[g] akaingia Ugiriki. **3** Na alipokuwa amekaa huko kwa miezi mitatu, kwa sababu hila[h] ilikuwa imetungwa juu yake na Wayahudi alipokuwa karibu kusafiri kwenda Siria, akaamua kurudi kupitia Makedonia. **4** Hawa waliandamana naye, Sopatro[i] mwana wa Piro wa Beroya, Aristarko[j] na Sekundo wa Wathesalonike, na Gayo wa Derbe, na Timotheo,[k] na kutoka wilaya ya Asia Tikiko[l] na Trofimo.[m] **5** Hao wakatangulia, wakatungojea huko Troa;[n] **6** lakini sisi tukaanza kusafiri baharini kutoka Filipi baada ya siku za keki zisizo na chachu,[o] nasi tukawafikia huko Troa[p] katika muda wa siku tano; na huko tukakaa siku saba.

SURA 19
a Mdo 21:34
b Mdo 19:28
c Met 15:18
d Met 14:29
e Mdo 19:24

Safu ya 2
a Mdo 17:34
b Mdo 13:7
Mdo 18:12
c Mhu 9:17
d Mdo 19:32

SURA 20
e 2Ko 2:13
f 1Ko 16:5
1Ti 1:3
g Ro 12:8
h Mdo 23:16
Mdo 25:3
2Ko 11:26
i Ro 16:21
j Mdo 27:2
k Mdo 16:1
l Efe 6:21
Kol 4:7
2Ti 4:12
m Mdo 21:29
2Ti 4:20
n Mdo 16:11
o Kut 12:14
Kut 23:15
p 2Ti 4:13

7 Siku ya kwanza[a] ya juma,
tulipokuwa tumekusanyika pa-
moja ili kupata mlo, Paulo aka-
anza kuwahutubia, kwa kuwa
alipaswa kuondoka siku inayo-
fuata; naye akarefusha hotu-
ba yake mpaka katikati ya
usiku. **8** Kwa hiyo kulikuwa
na taa nyingi katika chumba
cha juu[b] tulipokuwa tumeku-
sanyika pamoja. **9** Kijana fu-
lani anayeitwa Eutiko, aliye-
kuwa ameketi dirishani, aka-
lala usingizi mzito huku Pau-
lo akiendelea kuongea, naye
akalemewa na usingizi, akaa-
nguka chini kutoka ghorofa ya
tatu akaokotwa akiwa ameku-
fa. **10** Lakini Paulo akashu-
ka kutoka ghorofani, akajitu-
pa juu yake[c] akamkumbatia na
kusema: "Acheni kufanya ke-
lele, kwa maana nafsi yake
imo ndani yake."[d] **11** Akapa-
nda ghorofani, akapata mlo na
kula chakula, na baada ya kuo-
ngea kwa muda mrefu, mpaka
mapambazuko, mwishowe aka-
ondoka. **12** Basi wakamchu-
kua huyo mvulana akiwa hai
wakafarijiwa kupita kiasi.

13 Sasa tukaenda kwenye
mashua na kusafiri mpaka Aso,
ambako tulikusudia kumpa-
ndisha Paulo chomboni, kwa
maana, baada ya kutoa ma-
agizo hayo, yeye mwenyewe
alikusudia kwenda kwa mi-
guu. **14** Kwa hiyo alipotufi-
kia katika Aso, tukampandisha
chomboni na kwenda mpaka
Mitilene; **15** tukasafiri kuto-
ka huko siku iliyofuata, tuka-
fika upande wa pili wa Kio, la-
kini siku iliyofuata tukafika
Samo, na siku iliyofuata hiyo
tukafika Mileto. **16** Kwa ma-
ana Paulo alikuwa ameamua
kusafiri kupita Efeso,[a] ili asitu-
mie wakati wowote katika wila-
ya ya Asia; kwa maana aliku-
wa akifanya haraka afike Yeru-
salemu[b] siku ya sherehe ya Pe-
ntekoste kama kwa vyovyote
angeweza.

17 Hata hivyo, kutoka Mile-
to akatuma watu kwenda Efe-
so na kuwaita wanaume waze-
e[c] wa hilo kutaniko waje.
18 Walipofika kwake akawaam-
bia: "Ninyi mnajua vema ji-
nsi tangu siku ya kwanza nili-
yokanyaga wilaya ya Asia[d] ni-
livyokuwa pamoja nanyi wa-
kati wote,[e] **19** nikimtumikia[f]
Bwana nikiwa na unyenyeke-
vu mkubwa zaidi wa akili[g] na
machozi na majaribu yaliyo-
nipata kwa hila[h] za Wayahu-
di; **20** wakati uleule sikue-
puka kuwaambia ninyi lolote
kati ya mambo yenye faida wala
kuwafundisha[i] ninyi hadhara-
ni na nyumba[j] kwa nyumba.
21 Lakini nilitoa ushahidi[k] ki-
kamili kwa Wayahudi na Wagi-
riki pia juu ya toba[l] kwa Mu-
ngu na imani katika Bwana
wetu Yesu. **22** Na sasa, ta-
zameni! nikiwa nimefungwa
katika roho,[m] ninafunga safari
kwenda Yerusalemu, ijapoku-
wa sijui mambo yatakayonipa-
ta katika jiji hilo, **23** ila kwa-
mba kutoka jiji mpaka jiji roho
takatifu[n] inatoa ushahidi kwa-
ngu kwa kurudiarudia inapo-
sema kwamba vifungo na dhi-
ki vinaningojea.[o] **24** Hata hi-
yo, siifanyi nafsi yangu kuwa
kitu chenye thamani sana
kwangu,[p] kama tu ningepa-
ta kumaliza mwendo[q] wangu
na huduma[r] niliyopokea[s] kuto-
ka kwa Bwana Yesu, kutoa
ushahidi kamili kuhusu habari

SURA 20

a 1Ko 16:2
b Mdo 1:13
c 1Fa 17:21
2Fa 4:34
d Mt 9:24
Mk 5:39
Yoh 11:40
Mdo 9:40

Safu ya 2

a Mdo 18:21
b Mdo 21:4
Mdo 24:17
c Mdo 11:30
d Mdo 16:6
e Mdo 19:10
f 2Ko 11:27
g 1Ko 15:9
1Th 2:6
1Pe 5:3
h Mdo 9:24
Mdo 20:3
i Mt 28:20
Mdo 20:27
2Ti 4:2
j Mdo 5:42
k Mdo 18:5
l Mk 1:15
Lu 24:47
Mdo 2:38
m Mdo 19:21
n Mdo 21:4
Mdo 21:11
o Mdo 9:16
p Ro 8:35
2Ko 4:16
q 2Ti 4:7
r 2Ko 4:1
2Ko 5:18
s Ga 1:1

njema ya fadhili zisizostahiliwa za Mungu.[a]

25 "Na sasa, tazameni! ninajua kwamba ninyi nyote ambao nilienda kati yenu nikihubiri juu ya ufalme hamtauona uso wangu tena. **26** Kwa sababu hiyo ninawaita ninyi kuona ushahidi leo hii kwamba mimi ni safi kutokana na damu[b] ya watu wote, **27** kwa maana sikuepuka kuwaambia ninyi mashauri[c] yote ya Mungu. **28** Jiangalieni[d] ninyi wenyewe[e] na kundi lote,[f] ambalo roho takatifu imewaweka ninyi rasmi kuwa waangalizi[g] kati yake, kulichunga kutaniko la Mungu,[h] ambalo alilinunua kwa damu[i] ya Mwana wake mwenyewe. **29** Ninajua kwamba baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu[j] wenye kukandamiza wataingia katikati yenu nao hawatalitendea kundi kwa wororo, **30** na kutoka katikati yenu ninyi wenyewe watu watasimama na kusema mambo yaliyopotoka[k] ili kuwavuta wanafunzi wawafuate wao wenyewe.[l]

31 "Kwa hiyo endeleeni kukesha, na kukumbuka akilini kwamba kwa miaka mitatu,[m] usiku na mchana, sikuacha kumwonya[n] kila mmoja kwa machozi. **32** Na sasa ninawaweka ninyi mikononi mwa Mungu[o] na kwa neno la fadhili zake zisizostahiliwa, neno ambalo linaweza kuwajenga[p] na kuwapa urithi kati ya wale wote waliotakaswa.[q] **33** Sikutamani fedha au dhahabu au vazi la mtu.[r] **34** Ninyi wenyewe mnajua kwamba mikono hii imehudumia mahitaji yangu[s] na ya wale walio pamoja nami. **35** Nimewaonyesha ninyi wazi katika mambo yote kwamba kwa kufanya kazi[a] kwa bidii hivyo ni lazima mwasaidie wale walio dhaifu,[b] na lazima myakumbuke maneno ya Bwana Yesu, aliposema, 'Kuna furaha zaidi katika kutoa[c] kuliko ilivyo katika kupokea.'"

36 Alipokuwa amesema mambo haya, akapiga magoti[d] pamoja nao wote na kusali. **37** Kwa kweli, wote wakalia sana, nao wakamwangukia Paulo shingoni[e] na kumbusu[f] kwa wororo, **38** kwa sababu waliumizwa hasa na neno alilosema kwamba hawangemwona uso[g] wake tena. Basi wakaanza kumsindikiza[h] mpaka kwenye mashua.

21 Sasa tulipokuwa tumejiondoa kwao na kusafiri baharini, tulikwenda kwa mwendo wa moja kwa moja tukaja mpaka Kosi, lakini siku iliyofuata tukaja mpaka Rode, na kutoka huko mpaka Patara. **2** Na tulipokuwa tumepata mashua iliyokuwa ikivuka kwenda Foinike, tukapanda ndani, tukasafiri kwenda zetu. **3** Baada ya kuja mahali tulipoweza kuona kisiwa cha Kipro[i] tukakiacha nyuma upande wa kushoto, tukasafiri mpaka Siria,[j] tukafika Tiro, kwa maana mashua ilipaswa ipakue shehena yake huko.[k] **4** Baada ya kuwatafuta, tuliwapata wanafunzi na kukaa huko siku saba. Lakini kupitia roho[l] wakarudiarudia kumwambia Paulo asikanyage Yerusalemu. **5** Kwa hiyo tulipokuwa tumekamilisha hizo siku, tukatoka na kuanza kwenda; lakini hao wote, pamoja na wanawake na watoto, wakatupeleka mpaka nje ya jiji. Tu-

SURA 20
a 2Ko 6:1
b Eze 33:8
Mdo 18:6
2Ko 7:2
c Mt 28:20
Yoh 15:15
d Kol 4:17
1Ti 4:16
e 1Ti 3:2
f Met 27:23
g 1Ti 3:1
Tit 1:5
Ebr 13:17
h Yoh 21:15
Efe 4:11
1Pe 5:2
i Mt 26:28
Yoh 6:54
1Yo 1:7
j Isa 56:11
Mt 7:15
2Th 2:3
2Pe 2:1
k 2Ti 4:3
l Ga 4:17
1Ti 4:1
1Yo 2:19
m Mdo 19:10
n 2Ko 2:4
1Th 2:11
o Mdo 14:23
p Ro 16:25
q Kum 33:3
Efe 1:18
Kol 1:12
r 1Sa 12:3
Mt 10:8
1Ko 9:12
2Ko 7:2
Tit 1:7
s Mdo 18:3
1Ko 4:12
1Th 2:9

Safu ya 2
a Efe 4:28
1Th 4:11
2Th 3:8
b Ro 15:1
c Met 19:17
Mt 10:8
Lu 6:38
d Mdo 21:5
e Mwa 45:14
f Ro 16:16
g Mdo 20:25
h Mdo 15:3

SURA 21
i Mdo 15:39
j Mdo 20:3
k Mdo 27:10
l Mdo 21:11
Mdo 21:12

kapiga magoti[a] pwani, tukasali
6 na kuagana,[b] nasi tukapanda
ndani ya mashua lakini wao wa-
karudi nyumbani kwao.

7 Ndipo tukakamilisha safa-
ri ya baharini kutoka Tiro tu-
kafika Tolemai, nasi tukawasalimu akina ndugu na kukaa siku
moja pamoja nao. **8** Siku ili-
yofuata tukaondoka tukafika
Kaisaria,[c] nasi tukaingia kati-
ka nyumba ya Filipo mweneza-injili, aliyekuwa mmoja wa
wale watu saba,[d] nasi tukakaa
pamoja naye. **9** Mtu huyu ali-
kuwa na binti wanne, mabiki-
ra, waliotoa unabii.[e] **10** Laki-
ni tulipokuwa tukikaa siku
kadhaa, nabii fulani anayei-
twa Agabo[f] akashuka kutoka
Yudea, **11** naye akaja maha-
li tulipokuwa na kuuchukua
mshipi wa Paulo, akafunga mi-
guu na mikono yake mwenye-
we na kusema: "Hivi ndivyo ina-
vyosema roho takatifu, 'Mwa-
namume ambaye mshipi huu ni
wake, Wayahudi watamfunga[g]
hivi katika Yerusalemu na ku-
mtia[h] mikononi mwa watu wa
mataifa.'" **12** Sasa tuliposikia
jambo hilo, sisi na pia watu wa
mahali hapo tukaanza kumsihi
asipande[i] kwenda Yerusalemu.
13 Ndipo Paulo akajibu: "Mna-
fanya nini kwa kulia[j] na ku-
nifanya dhaifu moyoni?[k] Muwe
na hakika, niko tayari si kufu-
ngwa tu bali pia kufa[l] Yerusa-
lemu kwa ajili ya jina la Bwa-
na Yesu." **14** Alipokataa ku-
shawishika, tukakubali kimya-
kimya maneno haya: "Mapenzi[m]
ya Yehova na yatendeke."

15 Sasa baada ya siku hizo
tukajitayarisha kwa ajili ya
safari, tukaanza kupanda kwe-
nda Yerusalemu.[n] **16** Laki-
ni wengine kati ya wanafunzi
kutoka Kaisaria[a] wakaenda pa-
moja nasi pia, ili kutuleta kwa
mtu ambaye nyumbani mwake
tulipaswa kukaribishwa, Mna-
soni wa Kipro, mwanafunzi wa
zamani. **17** Tulipoingia Yeru-
salemu,[b] akina ndugu wakatu-
karibisha kwa furaha.[c] **18** La-
kini siku iliyofuata Paulo akai-
ngia pamoja nasi kwa Yakobo;[d]
na wanaume wote wazee wali-
kuwapo. **19** Naye akawasali-
mu na kuanza kusimulia[e] kirefu
juu ya mambo ambayo Mungu
alifanya katikati ya mataifa ku-
pitia kwa huduma yake.[f]

20 Baada ya kusikia jambo
hilo wakaanza kumtukuza Mu-
ngu, nao wakamwambia: "Una-
ona, ndugu, jinsi kulivyo na
maelfu mengi ya waamini wa-
lio kati ya Wayahudi; nao wote
ni wenye bidii kuhusu Sheria.[g]
21 Lakini wamesikia uvumi
ukitolewa juu yako kwamba
wewe umekuwa ukiwafundi-
sha Wayahudi wote kati ya ma-
taifa uasi-imani wa kumwacha
Musa,[h] ukiwaambia wasiwa-
tahiri[i] watoto wao wala kujie-
ndesha katika desturi za ki-
sherehe. **22** Basi, ni nini ki-
nachopaswa kufanywa juu ya
hilo? Kwa vyovyote vile wata-
sikia umefika. **23** Kwa hiyo
fanya jambo hili tunalokuam-
bia: Tuna wanaume wanne
wenye nadhiri juu yao wenye-
we. **24** Wachukue watu hawa
pamoja nawe[j] ujitakase ki-
sherehe pamoja nao na kuwa-
gharimia,[k] ili wapate kunyole-
wa[l] vichwa vyao. Na kwa hiyo
kila mtu atajua kwamba uvu-
mi mwingi walioambiwa juu
yako si kitu, bali kwamba una-
tembea kwa utaratibu, wewe

SURA 21

a Ezr 9:5
Mdo 9:40
Mdo 20:36
b Mdo 18:21
c Mdo 18:22
d Mdo 6:5
e Yoe 2:28
Mdo 2:17
1Ko 11:5
f Mdo 11:28
g Mdo 20:23
Mdo 21:33
h Mdo 9:16
i Mt 16:22
j Mdo 20:24
k Kum 20:8
l 2Ko 4:10
2Ti 4:6
m 1Sa 3:18
Mt 26:42
n Ro 15:25

Safu ya 2

a Mdo 18:22
b Mdo 24:11
c Mdo 15:4
d Mdo 12:17
Mdo 15:13
Ga 1:19
Ga 2:9
Yak 1:1
e Mdo 11:4
Mdo 14:27
f Mdo 15:12
Ro 15:18
g Mdo 15:1
Mdo 22:3
Ro 10:2
Ga 1:14
h Mdo 6:14
Ga 5:1
i Ro 2:28
1Ko 7:19
j Hes 6:2
k Hes 6:14
Hes 6:15
Hes 6:17
l Hes 6:18
Mdo 18:18

mwenyewe pia ukishika Sheria.[a] **25** Kwa habari ya wale
waamini kutoka kati ya mataifa, tumetuma watu, tukitoa
uamuzi wetu kwamba wanapaswa kujiepusha na vitu vilivyo-
tolewa dhabihu kwa sanamu[b] na pia damu[c] na vitu vilivyo-
nyongwa,[d] na uasherati."[e]
26 Ndipo Paulo akawachukua wanaume hao pamoja naye
siku iliyofuata akajitakasa kisherehe pamoja nao[f] na kuingia
ndani ya hekalu, kutoa tarifa juu ya siku ambazo zinge-
timizwa[g] kwa huo utakaso wa kisherehe, mpaka toleo[h] litole-
we kwa ajili ya kila mmoja wao.[i]
27 Sasa zile siku saba[j] zilipokuwa karibu kumalizika, Wa-
yahudi kutoka Asia walipomwona katika hekalu wakaanza
kuuvuruga umati wote,[k] nao wakamkamata, **28** wa-
kipaaza sauti: "Wanaume wa Israeli, saidieni! Huyu ndi-
ye mwanamume anayefundisha kila mtu kila mahali dhi-
di ya watu[l] na Sheria na mahali hapa na, zaidi ya hayo,
hata aliwaingiza Wagiriki katika hekalu naye amepatia una-
jisi mahali hapa patakatifu."[m]
29 Kwa maana hapo kwanza walikuwa wamemwona Trofi-
mo[n] Mwefeso katika jiji akiwa pamoja naye, lakini wali-
kuwa wakiwazia Paulo alikuwa amemwingiza katika hekalu.
30 Na jiji lote likawa na mchafuko,[o] na watu wakaanza ku-
kimbia pamoja; nao wakamkamata Paulo wakamkokota nje
ya hekalu.[p] Na mara moja milango ikafungwa. **31** Na wa-
lipokuwa wakitafuta kumuua, kiongozi wa kikosi cha aska-
ri-jeshi akaletewa habari kwa-

SURA 21

a 1Ko 9:20
b Mwa 35:2
Kut 34:15
Mdo 15:29
c Mwa 9:4
Law 3:17
Law 17:10
Kum 12:23
1Sa 14:32
d Law 17:13
e 1Ko 6:9
Kol 3:5
1Th 4:3
1Pe 4:3
f Mdo 24:18
1Ko 9:20
g Hes 6:5
h Hes 6:19
i Hes 6:21
j Hes 6:9
k Mdo 19:29
l Mdo 24:5
m Mdo 24:6
n Mdo 20:4
2Ti 4:20
o Mdo 17:5
p Mdo 26:21

Safu ya 2

a Mdo 21:27
b Mdo 23:27
c Mdo 23:26
d Mdo 20:23
Mdo 21:11
Efe 6:20
e Mdo 19:32
f Mdo 22:24
g Lu 23:18
Yoh 19:15
Mdo 22:22
h Mdo 5:36
i Flp 3:5
j Mdo 9:11
Mdo 22:3

mba Yerusalemu lote lilikuwa katika mvurugo;[a] **32** naye
mara moja akachukua askari-jeshi na maofisa-jeshi na kuwa-
kimbilia huko chini.[b] Walipomwona kiongozi huyo wa kije-
shi[c] na askari-jeshi, wakaacha kumpiga Paulo.
33 Ndipo kiongozi wa kijeshi akaja karibu akamkamata
na kutoa amri afungwe minyororo miwili;[d] naye akaanza
kuuliza huyo ni nani na alikuwa amefanya nini. **34** Lakini
wengine katika umati wakaanza kupaaza sauti kuhusu ja-
mbo moja, na wengine kuhusu lingine.[e] Kwa hiyo, kwa kuwa
hangeweza kujua jambo lolote la hakika kwa sababu ya
fujo hizo, akaamuru aletwe kwenye makao ya askari-je-
shi.[f] **35** Lakini alipofika juu ya ngazi, akachukuliwa na wale
askari-jeshi kwa sababu ya jeuri ya umati; **36** kwa maana
umati wa watu uliendelea kufuata, ukipaaza sauti: "Mwondo-
lee mbali!"[g]
37 Na alipokuwa karibu kuingizwa katika makao ya aska-
ri-jeshi, Paulo akamwambia kiongozi wa kijeshi: "Je, nina-
ruhusiwa kukuambia jambo fulani?" Akasema: "Je, unawe-
za kusema Kigiriki? **38** Je, kwa kweli wewe si yule Mmi-
sri ambaye kabla ya siku hizi alichochea uasi[h] na kuwaongo-
za kuingia nyikani wale wanaume elfu nne wenye kutumia
visu?" **39** Ndipo Paulo akasema: "Mimi, kwa kweli, ni Mya-
hudi[i] wa Tarso[j] katika Kilikia, raia wa jiji ambalo si lenye ku-
kosa umashuhuri. Kwa hiyo ninakuomba, uniruhusu nise-
me na watu hawa." **40** Baada

ya kutoa ruhusa, Paulo, akiwa
amesimama juu ya ngazi, aka-
wapungia[a] watu mkono wake.
Kulipokuwa na kimya kiku-
bwa, akawahutubia kwa lugha
ya Kiebrania,[b] akisema:

22 "Wanaume, akina ndu-
gu[c] na akina baba, siki-
eni kujitetea[d] kwangu mbele
yenu sasa." **2** (Basi, waliposi-
kia alikuwa akisema nao kati-
ka lugha ya Kiebrania,[e] wa-
kakaa kimya hata zaidi, naye
akasema:) **3** "Mimi ni Mya-
hudi,[f] aliyezaliwa katika Tar-
so ya Kilikia,[g] lakini aliyeeli-
mishwa katika jiji hili miguu-
ni pa Gamalieli,[h] nikiwa nime-
fundishwa kwa usahihi[i] kabisa
Sheria ya mababu, nikiwa mwe-
nye bidii[j] kuhusu Mungu kama
vile ninyi nyote mlivyo leo hii.
4 Nami niliitesa Njia hii mpaka
kifo,[k] nikifunga na kutia mage-
rezani[l] wanaume na wanawake
pia, **5** kama ambavyo kuhani
mkuu na pia kusanyiko lote la
wanaume wazee[m] wanavyowe-
za kunitolea ushahidi. Kutoka
kwao nilipata pia barua[n] nizi-
peleke kwa akina ndugu kati-
ka Damasko, nami nilikuwa ni-
naenda kuwaleta wale waliokuwa
huko pia mpaka Yerusalemu
wakiwa wamefungwa ili waa-
dhibiwe.

6 "Lakini nilipokuwa nikisa-
firi na kukaribia Damasko, kari-
bu katikati ya mchana, kwa gha-
fula nuru kubwa kutoka mbi-
nguni ikamulika kunizungu-
ka,[o] **7** nami nikaanguka chini
na kusikia sauti ikiniambia, 'Sa-
uli, Sauli, kwa nini unanitesa?'[p]
8 Nikajibu, 'Wewe ni nani, Bwa-
na?' Naye akaniambia, 'Mimi ni
Yesu Mnazareti, ambaye unate-
sa.'[q] **9** Basi watu waliokuwa

SURA 21

a Mdo 13:16
Mdo 19:33
b Mdo 26:14

SURA 22

c Mdo 7:2
d Flp 1:7
1Pe 3:15
e Mdo 21:40
f Mdo 26:5
Ro 11:1
g Mdo 21:39
Mdo 23:34
h Mdo 5:34
i Mdo 26:5
j Ga 1:14
Flp 3:6
k Mdo 8:3
Mdo 9:2
1Ti 1:13
l Mdo 26:10
m Mdo 4:23
n Mdo 9:2
o Mdo 9:3
Mdo 26:13
p Mdo 9:4
Mdo 26:14
q Yoh 18:5
Mdo 9:5
Mdo 26:15

Safu ya 2

a Da 10:7
b Mdo 9:7
c Lu 3:10
Mdo 16:30
d Mdo 26:16
e Mdo 9:8
f Mdo 10:22
1Ti 3:7
g Mdo 9:17
h Mdo 3:13
Mdo 5:30
i Mdo 9:15
Ga 1:15
j 1Ko 9:1
1Ko 15:8
k Mdo 3:14
Ebr 7:26
l 1Ko 11:23
Ga 1:12
m Mdo 4:20
Mdo 23:11
Mdo 26:16
n Mdo 9:18
o Isa 1:16
1Ko 6:11
Tit 3:5
Ebr 10:22
1Yo 1:7
Ufu 1:5
p Mdo 10:43
q Mdo 9:26
Ga 1:18
r 2Ko 12:1
s Mdo 9:29

pamoja nami,[a] kwa kweli, waka-
iona nuru hiyo lakini hawakui-
sikia sauti ya mwenye kusema
nami.[b] **10** Ndipo nikasema,
'Nitafanya nini,[c] Bwana?' Bwa-
na akaniambia, 'Simama, ondo-
ka uende Damasko, na huko uta-
ambiwa kila kitu ambacho ume-
wekewa kufanya.'[d] **11** Lakini
kwa kuwa singeweza kuona
kitu chochote kwa sababu ya
utukufu wa nuru hiyo, nikafi-
ka Damasko, nikiwa ninaongo-
zwa kwa mkono wa wale walio-
kuwa pamoja nami.[e]

12 "Basi Anania, mwana-
mume fulani mwenye kumhe-
shimu Mungu kulingana na
Sheria, mwenye kushuhudiwa
vema[f] na Wayahudi wote walio-
kuwa wakikaa huko, **13** aka-
ja kwangu, akasimama kando
yangu, akaniambia, 'Sauli, ndu-
gu, pata kuona tena!'[g] Nami ni-
katazama juu kumwelekea saa
ileile. **14** Akasema, 'Mungu
wa mababu[h] zetu amekucha-
gua[i] upate kujua mapenzi yake
na kumwona[j] yule Aliye mwa-
dilifu[k] na kuisikia sauti ya ki-
nywa chake,[l] **15** kwa sababu
unapaswa kuwa shahidi kwa
ajili yake kwa watu wote juu ya
mambo ambayo umeona na ku-
sikia.[m] **16** Na sasa kwa nini
unakawia? Simama, ubatizwe[n]
na uoshe[o] dhambi zako kwa ku-
liitia jina lake.'[p]

17 "Lakini nilipokuwa nime-
rudi Yerusalemu[q] na nikiwa
ninasali hekaluni, nikapata njo-
zi[r] **18** na kumwona akiniam-
bia, 'Fanya upesi uondoke Ye-
rusalemu haraka, kwa sababu
hawatakubali[s] ushahidi wako
kunihusu.' **19** Nami nikase-
ma, 'Bwana, wao wenyewe wa-
najua vema kwamba nilikuwa

nikiwatia gerezani[a] na kuwapiga viboko katika sinagogi moja baada ya lingine wale wenye kukuamini;[b] **20** na wakati damu ya Stefano[c] shahidi wako ilipokuwa ikimwagwa, mimi mwenyewe nilikuwa pia nimesimama kando nikikubaliana[d] na jambo hilo na kuyalinda mavazi ya nje ya hao waliokuwa wakimuua.' **21** Na bado akaniambia, 'Ondoka uende, kwa sababu nitakutuma mbali sana kwa mataifa.'"[e]

22 Basi wakaendelea kumsikiliza mpaka kwenye neno hili, nao wakapaaza sauti zao, wakisema: "Mwondolee mbali mtu wa namna hiyo duniani, kwa maana yeye hakufaa kuishi!"[f] **23** Na kwa sababu walikuwa wakipaaza sauti na kutupa mavazi yao ya nje huku na huku na kurusha mavumbi hewani,[g] **24** yule kiongozi wa kijeshi akaagiza aingizwe katika makao ya askari-jeshi na kusema anapaswa kuhojiwa kwa kupigwa mijeledi, ili apate kujua kabisa ni kwa sababu gani walikuwa wakipaaza sauti[h] juu yake kwa njia hii. **25** Lakini walipokuwa wamemnyoosha ili apigwe mijeledi, Paulo akamwambia ofisa-jeshi aliyekuwa amesimama hapo: "Je, ni halali kwa ninyi watu kumpiga mijeledi mtu ambaye ni Mroma[i] na ambaye hajahukumiwa kuwa mwenye hatia?" **26** Basi, huyo ofisa-jeshi aliposikia jambo hilo, akaenda mpaka kwa kiongozi wa kijeshi na kueleza, akisema: "Unakusudia kufanya nini? Kwani, mtu huyu ni Mroma." **27** Kwa hiyo kiongozi wa kijeshi akakaribia na kumwambia: "Niambie, Je, wewe ni Mroma?"[a] Akasema: "Ndiyo." **28** Kiongozi wa kijeshi akajibu: "Mimi nilinunua haki hizo za kuwa raia kwa pesa nyingi." Paulo akasema: "Lakini mimi, hata nilizaliwa[b] nazo."

29 Kwa hiyo, mara moja watu waliokuwa karibu kumhoji kwa kumtesa wakaondoka kwake; na kiongozi wa kijeshi akaogopa alipohakikisha kwamba alikuwa Mroma[c] na kwamba alikuwa amemfunga.

30 Kwa hiyo, siku iliyofuata, kwa kuwa alitaka kujua kwa hakika ni kwa nini hasa alikuwa akishtakiwa na Wayahudi, akamfungua na kuwaamuru wakuu wa makuhani na Sanhedrini yote wakusanyike. Naye akamleta Paulo chini na kumsimamisha katikati yao.[d]

23 Paulo akaikazia macho Sanhedrini, akasema: "Wanaume, akina ndugu, nimejiendesha mbele za Mungu kwa dhamiri[e] iliyo safi kikamilifu mpaka leo hii." **2** Ndipo kuhani mkuu Anania akawaagiza wale waliosimama kando yake wampige[f] kinywani. **3** Ndipo Paulo akamwambia: "Mungu atakupiga wewe, ewe ukuta uliopakwa chokaa.[g] Je, wakati uleule mmoja unaketi kunihukumu kupatana na Sheria[h] na, kwa kuvunja Sheria,[i] unaamuru nipigwe?" **4** Wale waliosimama kando wakasema: "Je, wewe unamtukana kuhani mkuu wa Mungu?" **5** Na Paulo akasema: "Akina ndugu, sikujua yeye ni kuhani mkuu. Kwa maana imeandikwa, 'Usiseme vibaya juu ya mtawala wa watu wako.'"[j]

6 Sasa Paulo alipojua kwa-

SURA 22
a Mdo 8:3
b Mt 10:17
c Mdo 7:58
d Mdo 8:1
1Ti 1:15
e Mdo 9:15
Mdo 13:2
Ro 1:5
Ro 11:13
Ga 2:7
1Ti 2:7
f Mdo 21:36
Mdo 23:14
Mdo 25:24
g 2Sa 16:13
h Mdo 21:34
i Mdo 16:37
Mdo 23:27

Safu ya 2
a Mdo 23:27
b Mdo 16:37
c Mdo 16:38
Mdo 25:16
d Mt 10:17
Lu 21:12

SURA 23
e Mdo 24:16
2Ko 1:12
2Ti 1:3
Ebr 13:18
1Pe 3:16
f 1Fa 22:24
Yer 20:2
Yoh 18:22
g Mt 23:27
h Law 19:15
i Kum 25:1
Yoh 7:51
j Kut 22:28
Mhu 10:20

mba sehemu moja ilikuwa ya
Masadukayo[a] lakini ile nyi-
ngine ya Mafarisayo, akapaa-
za sauti katika Sanhedrini
hiyo: "Wanaume, akina ndu-
gu, mimi ni Farisayo,[b] mwa-
na wa Mafarisayo. Ninahuku-
miwa[c] juu ya tumaini la ufu-
fuo[d] wa wafu." **7** Kwa sababu
alisema jambo hilo, mtengano[e]
ukatokea kati ya Mafarisayo na
Masadukayo, na umati ukaga-
wanyika. **8** Kwa maana Ma-
sadukayo[f] husema hakuna ufu-
fuo[g] wala malaika wala roho,
lakini Mafarisayo huyatangaza
yote hadharani. **9** Kwa hiyo
watu wakaanza kupiga mayo-
we[h] kwa sauti kubwa, na wengi-
ne kati ya waandishi wa chama
cha Mafarisayo wakasimama
na kuanza kushindana vikali,
wakisema: "Sisi hatuoni kosa
lolote katika mtu huyu;[i] lakini
ikiwa roho au malaika alisema
naye,[j] —." **10** Basi mtengano
ulipokuwa mkubwa, kiongozi
wa kijeshi akaogopa kwamba
wangemrarua Paulo vipande-
vipande, naye akaamuru jeshi
la askari[k] lishuke liende ku-
mnyakua kutoka katikati yao
na kumleta ndani ya makao ya
askari-jeshi.[l]

11 Lakini usiku uliofuata
Bwana akasimama kando yake[m]
na kusema: "Jipe moyo![n] Kwa
maana kama vile ambavyo ume-
kuwa ukitoa ushahidi[o] kamili
katika Yerusalemu juu ya ma-
mbo yanayonihusu, vivyo hivyo
utatoa ushahidi katika Roma
pia."[p]

12 Sasa kulipokuwa mcha-
na, Wayahudi wakafanya hila[q]
na kujifunga wenyewe kwa la-
ana,[r] wakisema hawangeku-
la wala kunywa mpaka wawe

SURA 23

a Mdo 4:1

b Mdo 26:5
Flp 3:5

c Mdo 28:20

d Mdo 24:21

e Mt 22:23

f Mk 12:18

g Lu 20:27

h Mt 8:29

i Lu 23:4
Mdo 25:25

j Mdo 22:7
Mdo 22:17

k Mdo 21:32

l Mdo 22:24

m Mdo 27:23

n Mdo 18:9
Mdo 27:24

o Mdo 20:21

p Mdo 28:23
Mdo 28:30
Ro 1:15

q Mdo 25:3

r Mdo 23:21

Safu ya 2

a Zb 31:13

b Mhu 5:8

c Mdo 23:20

d Mdo 25:3

e Mdo 9:24

f Mdo 23:16

g Mdo 23:15

wamemuua Paulo.[a] **13** Kuli-
kuwa na zaidi ya watu 40 wa-
liofanya hila hiyo iliyofungwa
kwa kiapo; **14** nao wakaenda
kwa wakuu[b] wa makuhani
na wanaume wazee na kusema:
"Sisi tumejifunga wenyewe
chini ya laana kwa uzito kuto-
onja chakula mpaka tuwe tu-
memuua Paulo. **15** Kwa hiyo,
basi, ninyi pamoja na Sanhe-
drini mfanyeni kiongozi wa ki-
jeshi aelewe ni kwa nini ana-
paswa kumshusha chini kwe-
nu kana kwamba mnakusudia
kuhakikisha kwa usahihi zaidi
mambo yanayomhusu.[c] Lakini
kabla hajafika karibu tutakuwa
tayari kumuua."[d]

16 Hata hivyo, mwana wa
dada ya Paulo akasikia juu
ya kuvizia kwao,[e] naye akaja
na kuingia katika makao
ya askari-jeshi hao akamwele-
za Paulo jambo hilo. **17** Basi
Paulo akamwita mmoja wa ma-
ofisa-jeshi na kusema: "Mpe-
leke kijana huyu kwa kiongo-
zi wa kijeshi, kwa maana ana
jambo fulani la kumweleza."
18 Kwa hiyo mtu huyu akam-
chukua na kumpeleka kwa ki-
ongozi wa kijeshi na kusema:
"Mfungwa Paulo aliniita na ku-
niomba nimlete kijana huyu
kwako, kwa kuwa ana jambo
la kukuambia." **19** Kiongozi
wa kijeshi akamshika[f] mkono,
akaondoka, na kuanza kumu-
uliza faraghani: "Unataka ku-
niambia nini?" **20** Akasema:
"Wayahudi wamepatana kuku-
omba umshushe Paulo kwenye
Sanhedrini kesho kana kwamba
wanakusudia kujua jambo fula-
ni kwa usahihi zaidi juu yake.[g]
21 Zaidi ya mambo yote, usiwa-
ache wakushawishi, kwa maana

wanaume wao zaidi ya 40 wanamvizia,[a] nao wamejifunga
wenyewe kwa laana kutokula wala kunywa mpaka wawe
wamemuua;[b] nao sasa wako tayari, wakingojea ahadi kutoka
kwako." **22** Kwa hiyo huyo kiongozi wa kijeshi akamwacha
huyo kijana aende baada ya kumwagiza: "Usipayuke-payuke
kwa yeyote kwamba umenieleza mambo hayo."

23 Naye akawaita watu fulani wawili kati ya maofisajeshi na kusema: "Tayarisheni askari-jeshi 200 ili waende
moja kwa moja mpaka Kaisaria, pia wapanda-farasi 70
na watu 200 wachukua-mikuki, saa tatu ya usiku. **24** Pia,
andaeni wanyama wa kubeba mizigo ili wampandishe Paulo
na kumpeleka salama kwa Feliksi gavana." **25** Naye akaandika barua ya namna hii:

26 "Klaudio Lisia kwa mtukufu, Gavana Feliksi:[c] Salamu!
27 Mwanamume huyu alikamatwa na Wayahudi nao walikuwa karibu kumuua, lakini nikaja ghafula nikiwa pamoja na jeshi la askari na kumwokoa,[d] kwa sababu nilipata
kujua kwamba yeye ni Mroma.[e]
28 Nami nikitaka kuhakikisha sababu waliyokuwa wakimshtakia, nikamleta ndani ya
Sanhedrini yao.[f] **29** Niliona ameshtakiwa juu ya maswali ya
Sheria yao,[g] lakini hajashtakiwa hata jambo moja la kustahili kifo au vifungo.[h] **30** Lakini kwa sababu hila[i] itakayofanywa juu ya mwanamume huyu imefunuliwa kwangu,
ninamtuma kwako mara moja, na kuwaamuru washtaki wamshtaki mbele yako."[j]

SURA 23
a Zb 10:9
Met 1:16
Isa 59:7
Mdo 9:23
2Ko 11:26
b Mdo 23:12
c Mdo 24:3
d Mdo 21:33
e Mdo 16:37
Mdo 22:25
f Mdo 22:30
g Mdo 18:15
Mdo 24:5
Mdo 25:19
h Mdo 26:31
i Mdo 23:16
Mdo 25:3
j Mdo 24:8
Mdo 25:5
Mdo 25:11

Safu ya 2
a Mdo 23:23
b Mdo 8:40
c Mdo 22:3
d Mdo 6:9
Mdo 21:39
e Mdo 24:1
Mdo 25:16

SURA 24
f Mdo 23:2
g Mdo 25:2
Mdo 25:15
h Mdo 23:26
i Zb 12:2
Zb 55:21
Met 26:28
j Mdo 23:26
k Mt 5:11
Mdo 16:20
Mdo 17:6
l Lu 23:2
Mdo 19:40

31 Kwa hiyo askari-jeshi[a]
hao wakamchukua Paulo kulingana na walivyoagizwa wakamleta wakati wa usiku mpaka Antipatri. **32** Siku iliyofuata wakaruhusu wapandafarasi waende pamoja naye,
nao wakarudi kwenye makao ya askari-jeshi. **33** Hao wapanda-farasi wakaingia katika Kaisaria[b] na kumkabidhi gavana hiyo barua na pia wakamleta Paulo mbele yake. **34** Basi
akaisoma na kuuliza alikuwa ametoka jimbo gani, akapata
kujua hakika[c] kwamba alikuwa ametoka Kilikia.[d] **35** "Nitasikia kesi yako vilivyo," akasema, "washtaki wako watakapofika pia."[e] Naye akaamuru kwamba awekwe chini ya
ulinzi katika jumba la kimaliki la Herode.

24 Siku tano baadaye kuhani mkuu Anania[f] akashuka pamoja na wanaume
fulani wazee na msemaji wa hadharani, Tertulo, nao wakamweleza[g] gavana[h] juu ya
Paulo. **2** Alipoitwa, Tertulo akaanza kumshtaki, akisema:

"Kwa kuwa tunaonea shangwe amani[i] kubwa kupitia
kwako na kwamba marekebisho yanatokea katika taifa hili
kupitia ufikirio wako wa kimbele, **3** nyakati zote na pia
mahali pote tunapokea mambo hayo, Ewe Mtukufu[j] Feliksi, kwa shukrani zilizo kubwa zaidi. **4** Lakini ili nisikuzuie zaidi, ninakuomba utusikie kwa ufupi kwa fadhili zako.
5 Kwa maana tumemwona mwanamume huyu kuwa mtu
msumbufu[k] na mwenye kufanya uchochezi wa uasi[l] kati ya
Wayahudi wote katika dunia

yote inayokaliwa na kuwa kiongozi mkuu wa madhehebu ya
Wanazareti,[a] **6** ambaye pia
alijaribu kulichafua hekalu[b] na
ambaye tulimkamata. **7** ——
8 Kutoka kwake wewe mwe-
nyewe unaweza kugundua kwa
kumhoji juu ya mambo haya
yote ambayo sisi tunamshtaki."

9 Ndipo Wayahudi pia waka-
jiunga katika shambulio hilo,
wakisisitiza kwamba mambo
hayo ndivyo yalivyo. **10** Na
Paulo, wakati gavana alipomto-
lea ishara aseme, akajibu:

"Kwa kujua vema kwamba
wewe umekuwa mwamuzi wa
taifa hili kwa miaka mingi,
mimi ninasema kwa utayari ka-
tika kujiteteа[c] juu ya mambo
yanayonihusu mimi mwenye-
we, **11** kwa kuwa wewe una-
weza kugundua kwamba kwa-
ngu mimi haijawa zaidi ya siku
kumi na mbili tangu nilipo-
panda kwenda kuabudu[d] kati-
ka Yerusalemu; **12** nao hawa-
kuniona katika hekalu[e] nikibi-
shana na mtu yeyote wala ni-
kifanya kikundi chenye ghasia[f]
kikimbie pamoja, ama katika
masinagogi ama kotekote kati-
ka jiji. **13** Wala hawawezi ku-
kuthibitishia[g] mambo wanayo-
nishtaki sasa hivi. **14** Lakini
ninakiri jambo hili kwako, kwa-
mba, kulingana na ile njia wa-
nayoiita 'madhehebu,' kwa na-
mna hii mimi ninatoa utumishi
mtakatifu kwa Mungu wa ma-
babu zangu,[h] kwa kuwa nina-
amini mambo yote yaliyo kati-
ka Sheria[i] na kuandikwa kati-
ka Manabii; **15** nami nina tu-
maini[j] kwa Mungu, tumaini
ambalo watu hawa pia wana-
lo, kwamba kutakuwa na ufu-
fuo[k] wa waadilifu[l] na wasio wa-

SURA 24

a Mt 2:23
Mdo 28:22
b Mdo 21:28
c 1Pe 3:15
d Mdo 21:26
e Mdo 25:8
f Mdo 21:28
g Mdo 25:7
h Kut 3:15
Mdo 3:13
Mdo 26:22
2Ti 1:3
i Kum 18:18
Mdo 28:23
Ro 3:21
j Mdo 23:6
k Isa 26:19
Da 12:2
Mt 22:31
Yoh 5:28
Yoh 11:25
Ufu 20:12
l Lu 14:14
Ebr 11:35

Safu ya 2

a Lu 23:43
b Da 6:5
Mdo 23:1
1Ko 4:4
Ebr 13:18
c Mdo 11:29
2Ko 8:4
d Mdo 21:26
e Mdo 23:30
Mdo 25:16
f Mdo 23:6
Mdo 28:20
g Mdo 23:24
h Mdo 9:2
Mdo 19:9
i Mdo 23:26
j Mdo 27:3
k Mdo 23:24
l Mdo 16:1
m Mt 10:18
1Pe 3:15

adilifu[a] pia. **16** Katika haba-
ri hii, kwa kweli, ninajizoeza
mwenyewe sikuzote kudhami-
ria[b] kutomkosea Mungu na wa-
nadamu. **17** Kwa hiyo baada
ya miaka kadhaa nilifika kule-
ta zawadi za rehema kwa taifa
langu, na matoleo.[c] **18** Ni-
lipokuwa nikishughulikia ma-
mbo haya wakanikuta nikiwa
nimetakaswa kisherehe kati-
ka hekalu,[d] lakini nikiwa bila
umati wala fujo. Lakini kuliku-
wa na Wayahudi fulani kutoka
wilaya ya Asia, **19** ambao wa-
napaswa kuwapo mbele yako
na kunishtaki ikiwa wana ja-
mbo lolote juu yangu.[e] **20** Au,
acha watu walio hapa wajise-
mee wenyewe ni kosa gani wali-
loona nilipokuwa nimesimama
mbele ya Sanhedrini, **21** ila
kwa habari ya neno hili moja
nililopaaza sauti nikiwa nimesi-
mama kati yao, 'Mimi ninahu-
kumiwa leo mbele yenu juu ya
ufufuo wa wafu!' "[f]

22 Hata hivyo, Feliksi,[g] aki-
jua kwa usahihi kabisa mambo
yanayoihusu Njia[h] hii, akaahiri-
sha kesi ya watu hao na kuse-
ma: "Wakati wowote Lisia[i] ki-
ongozi wa kijeshi atakapoku-
ja, nitaamua mambo haya ya-
nayowahusu ninyi." **23** Naye
akamwagiza ofisa-jeshi kwa-
mba mtu huyo atunzwe na awe
na starehe fulani ya kizuizini,
na kwamba asimkataze yeyote
kati ya watu wake kumhudu-
mia.[j]

24 Siku kadhaa baadaye Fe-
liksi[k] akafika pamoja na Drusi-
la mke wake, aliyekuwa Mya-
hudi,[l] naye akatuma watu ku-
mwita Paulo na kumsikiliza juu
ya imani katika Kristo Yesu.[m]
25 Lakini alipokuwa akiongea

juu ya uadilifu[a] na kujizuia[b] na
hukumu[c] itakayokuja, Feliksi
akaogopa na kujibu: "Kwa wa-
kati huu wa sasa ondoka ue-
nde, lakini nitakapopata wa-
kati unaofaa nitakuita tena."
26 Ingawa hivyo, wakati huo-
huo, alikuwa akitumaini Pau-
lo ampe pesa.[d] Kwa ajili ya hilo
akamwita mara nyingi hata za-
idi na akawa akiongea naye.[e]
27 Lakini, miaka miwili ilipo-
kuwa imepita, nafasi ya Felik-
si ilichukuliwa na Porkio Fes-
to; na kwa sababu Feliksi alita-
mani kupata kibali[f] cha Waya-
hudi, akamwacha Paulo akiwa
amefungwa.

25 Kwa hiyo Festo, baada
ya kuingia[g] katika cheo
cha serikali ya jimbo, siku
tatu baadaye alipanda kwe-
nda Yerusalemu kutoka Kaisa-
ria;[h] **2** na wakuu wa makuha-
ni na watu walio wakuu kati
ya Wayahudi wakamweleza[i]
mashtaka juu ya Paulo. Basi
wakaanza kumsihi, **3** wakiji-
ombea kibali dhidi ya mtu huyo
ili amwite aje mpaka Yerusa-
lemu, kwa kuwa walikuwa wa-
kivizia[j] ili kumuua barabarani.
4 Hata hivyo, Festo akajibu
kwamba Paulo alipaswa kuli-
ndwa katika Kaisaria na kwa-
mba yeye mwenyewe angeenda
huko hivi karibuni. **5** "Kwa
sababu hiyo acheni wale walio
na mamlaka kati yenu," akase-
ma, "washuke pamoja nami na
kumshtaki,[k] ikiwa kuna jambo
lolote lisilofaa juu ya mwana-
mume huyo."

6 Kwa hiyo alipokuwa ame-
kaa siku zisizozidi nane au
kumi kati yao, akashuka kwe-
nda Kaisaria, na siku iliyo-

SURA 24
a Ro 1:17
Ro 3:22
b Ga 5:23
2Pe 1:6
c Mt 12:18
Yoh 16:8
2Ko 5:10
Ufu 20:12
d Kut 23:8
Kum 16:19
Zb 26:10
Met 17:23
Isa 5:23
e Mk 6:20
f Met 29:25
Lu 23:25
Mdo 25:9

SURA 25
g Mdo 24:27
h Mdo 21:15
i Mdo 24:1
Mdo 25:15
j Zb 37:32
Met 1:16
Mdo 9:23
Mdo 14:5
Mdo 23:21
2Ko 11:26
k Mdo 25:16

Safu ya 2
a Yoh 19:13
Mdo 12:21
Mdo 25:17
b Mt 5:11
Lu 23:2
Mdo 24:5
c Mdo 24:12
Mdo 28:17
d Mdo 24:27
e Mdo 25:20
f Mdo 25:21
Mdo 26:32
g Mdo 28:17
h 1Pe 4:15
i Mdo 23:29
Mdo 26:31
j Mdo 25:21
Mdo 26:32
Mdo 28:19

fuata akaketi juu ya kiti cha
hukumu[a] na kuamuru Paulo
aingizwe ndani. **7** Alipofika,
Wayahudi waliokuwa wame-
shuka kutoka Yerusalemu wa-
kasimama kumzunguka huku
na huku, wakileta juu yake ma-
shtaka[b] mengi na mazito amba-
yo hawakuweza kuthibitisha.

8 Lakini Paulo akasema kwa
kujitetea: "Sijatenda dhambi yo-
yote juu ya Sheria ya Wayahudi
wala juu ya hekalu wala juu ya
Kaisari."[c] **9** Festo, akitamani
kupata kibali[d] cha Wayahudi,
akasema kwa kumjibu Paulo:
"Je, wewe ungetaka kupanda
kwenda Yerusalemu uhukumi-
we huko mbele yangu kuhu-
su mambo haya?"[e] **10** Lakini
Paulo akasema: "Mimi nimesi-
mama mbele ya kiti cha hu-
kumu cha Kaisari,[f] ambapo
ninapaswa kuhukumiwa. Si-
jawatendea Wayahudi kosa,[g]
kama vile wewe pia unavyogu-
ndua vema kabisa. **11** Ikiwa,
kwa upande mmoja, mimi ni
mkosaji[h] kwa kweli na nime-
fanya jambo lolote linalostahili
kifo,[i] sikatai kufa; ikiwa, kwa
upande mwingine, hakuna hata
moja la mambo hayo ambalo
watu hawa wananishtakia,
hakuna mtu anayeweza kuni-
kabidhi kwao ili kupata kiba-
li. Ninakata rufani kwa Kai-
sari!"[j] **12** Ndipo Festo, baa-
da ya kusema na kusanyiko
la washauri, akajibu: "Umeka-
ta rufani kwa Kaisari; utaenda
kwa Kaisari."

13 Basi siku kadhaa zili-
pokuwa zimepita, Agripa mfa-
lme na Bernike wakafika Ka-
isaria kwa ziara ya kumsali-
mu Festo. **14** Kwa kuwa wali-
kuwa wakikaa siku kadhaa

huko, Festo akaweka mbele ya
mfalme mambo yanayomhusu
Paulo, akisema:
"Kuna mwanamume fulani
ambaye Feliksi alimwacha aki-
wa mfungwa, **15** na nilipoku-
wa Yerusalemu wakuu wa ma-
kuhani na wanaume wazee wa
Wayahudi walileta habari[a] juu
yake, wakiomba hukumu ya
adhabu juu yake. **16** Lakini
nikawajibu kwamba si utaratibu
wa Kiroma kukabidhi mtu
yeyote ili kupata kibali ka-
bla ya mtu huyo aliyeshtaki-
wa kukutana uso kwa uso na
washtaki[b] wake na kupata na-
fasi ya kujitetea kuhusu mala-
lamishi. **17** Kwa hiyo walipo-
kuja pamoja hapa, sikukawia,
bali siku iliyofuata niliketi juu
ya kiti cha hukumu na kua-
muru mwanamume huyo aingi-
zwe ndani. **18** Waliposima-
ma, washtaki hawakutokeza
shtaka[c] juu ya mambo maovu
niliyokuwa nimedhani kumhu-
su. **19** Walikuwa tu na ma-
bishano fulani pamoja naye
kuhusu ibada[d] yao wenyewe
ya mungu na kuhusu mtu fu-
lani anayeitwa Yesu aliyekuwa
amekufa lakini ambaye Paulo
alikuwa akisisitiza kwamba ali-
kuwa hai.[e] **20** Kwa hiyo, niki-
wa nimefadhaishwa na bishano
juu ya mambo haya, niliende-
lea kuuliza kama angependa
kwenda mpaka Yerusalemu na
huko akahukumiwe kuhusu
mambo haya.[f] **21** Lakini Pau-
lo alipokata rufani[g] awekwe
kwa ajili ya uamuzi wa Mhe-
shimiwa, nikaamuru awekwe
mpaka nimtume kwa Kaisari."
22 Hapo Agripa akamwa-
mbia Festo: "Mimi mwenye-
we ningependa pia kumsikia
mtu huyo."[a] "Kesho," akasema,
"Utamsikia." **23** Kwa hiyo,
siku iliyofuata, Agripa na Ber-
nike wakaja kwa fahari[b] nyi-
ngi na kuingia katika chumba
cha baraza pamoja na viongo-
zi wa kijeshi na vilevile wanau-
me waheshimiwa katika jiji, na
Festo alipotoa amri, Paulo aka-
ingizwa ndani. **24** Naye Fe-
sto akasema: "Mfalme Agripa
na ninyi wanaume wote mlio-
po pamoja nasi, ninyi mnao-
na mtu huyu ambaye kuhusu
yeye umati wote wa Wayahudi
ukiwa pamoja umepeleka ombi
kwangu katika Yerusalemu na
hapa pia, ukipaaza sauti kwa-
mba hapaswi kuishi tena ka-
mwe.[c] **25** Lakini mimi nikao-
na hakuwa amefanya jambo lo-
lote linalostahili kifo.[d] Kwa
hiyo mwanamume huyu mwe-
nyewe alipokata rufani[e] kwa
Mheshimiwa, niliamua kumpe-
leka. **26** Lakini kuhusu yeye
sina jambo hakika la kumwa-
ndikia Bwana wangu. Kwa hiyo
nikamleta mbele yenu, na hasa
mbele yako wewe, Mfalme Agri-
pa, ili, baada ya kumhoji kihu-
kumu,[f] nipate jambo fulani la
kuandika. **27** Kwa maana li-
naonekana kuwa jambo lisilo la
akili kwangu kumpeleka mfu-
ngwa bila kuonyesha mashtaka
juu yake."

26 Agripa[g] akamwambia
Paulo: "Unaruhusiwa ku-
jitetea." Ndipo Paulo akanyo-
osha mkono[h] wake na kuanza
kujitetea:[i]
2 "Kuhusu mambo yote nina-
yoshtakiwa[j] na Wayahudi, Mfa-
lme Agripa, ninajihesabu mwe-
nyewe kuwa mwenye furaha
kwamba ninajitetea mbele yako
leo, **3** hasa kwa kuwa wewe

SURA 25
a Mdo 25:2
b Mdo 25:5
c Mdo 25:7
d Mdo 18:15
Mdo 23:29
e Mdo 22:8
f Mdo 25:9
g Mdo 25:11
Mdo 26:32
Mdo 28:19

Safu ya 2
a Mdo 9:15
b 1Pe 1:24
1Yo 2:16
c Mdo 22:22
d Mdo 23:29
Mdo 26:31
e Mdo 25:21
f Mdo 26:32

SURA 26
g Mdo 25:13
h Mdo 13:16
i Mdo 24:10
j Mdo 24:5

una ujuzi juu ya desturi[a] zote na
vilevile mabishano kati ya Wa-
yahudi. Kwa hiyo ninakuomba
unisikie kwa subira.
4 "Kwa kweli, juu ya mai-
sha[b] ya tangu ujana na ku-
endelea ambayo niliishi tangu
mwanzo kati ya taifa langu
na katika Yerusalemu, Waya-
hudi wote **5** ambao walini-
fahamu tangu mwanzo wana-
jua, kama tu wangetaka kutoa
ushahidi, kwamba kulingana
na usahihi kabisa wa madhe-
hebu[c] ya namna yetu ya iba-
da mimi niliishi nikiwa Farisa-
yo.[d] **6** Lakini sasa kwa saba-
bu ya tumaini[e] la ahadi[f] iliyo-
tolewa na Mungu kwa mababu
zetu nimeitwa kwenye huku-
mu; **7** lakini makabila yetu
kumi na mawili yanatumai-
ni kufikia utimizo wa ahadi hii
kwa kumtolea utumishi mta-
katifu kwa juhudi nyingi usi-
ku na mchana.[g] Kuhusu tuma-
ini hili ninashtakiwa[h] na Waya-
hudi, Ewe mfalme.
8 "Kwa nini mnaamua kwa-
mba ni jambo lisiloaminika
kwamba Mungu hufufua wafu?[i]
9 Mimi, kwa kweli nilifikiri
ndani yangu mwenyewe kwa-
mba ninapaswa kufanya ma-
tendo mengi ya upinzani
juu ya jina la Yesu Mnazareti;
10 ambayo, kwa kweli, niliya-
fanya katika Yerusalemu, na
wengi kati ya watakatifu nili-
wafunga gerezani,[j] kwa kuwa
nilikuwa nimepokea mamlaka
kutoka kwa wakuu wa maku-
hani;[k] na walipokuwa wana-
paswa kuuawa, mimi nilipiga
kura yangu dhidi yao. **11** Na
kwa kuwaadhibu nyakati nyi-
ngi katika masinagogi[l] yote ni-
lijaribu kuwalazimisha wakane
imani yao; na kwa kuwa nilikuwa nimejawa na wazimu kupita kiasi juu yao, nilifikia hatua ya kuwatesa hata katika majiji ya nje.
12 "Katikati ya jitihada hizo nilipokuwa nikisafiri kwenda Damasko[a] nikiwa na mamlaka na utume kutoka kwa wakuu wa makuhani, **13** katikati ya mchana niliona barabarani, Ee mfalme, nuru inayopita wangavu wa jua ikimulika kutoka mbinguni kunizunguka na kuwazunguka wale waliokuwa wakisafiri pamoja nami.[b] **14** Na sisi sote tulipokuwa tumeanguka chini nikasikia sauti ikiniambia katika lugha ya Kiebrania, 'Sauli, Sauli, kwa nini unanitesa? Kuendelea kuipiga teke michokoo hufanya iwe vigumu kwako.'[c] **15** Lakini nikasema, 'Wewe ni nani, Bwana?' Naye Bwana akasema, 'Mimi ni Yesu, ambaye unatesa.[d] **16** Hata hivyo, inuka usimame kwa miguu yako.[e] Kwa maana nimejionyesha kwako kwa sababu hii, ili nikuchague wewe uwe mtumishi na shahidi[f] wa mambo ambayo umeona na pia mambo nitakayokuonyesha juu yangu; **17** huku mimi nikikukomboa kutoka kwa watu hawa na kutoka katika mataifa, ambao kwao ninakutuma wewe,[g] **18** kufungua macho[h] yao, kuwageuza kutoka katika giza[i] kuingia katika nuru[j] na kutoka katika mamlaka ya Shetani[k] na kumgeukia Mungu, kusudi wapokee msamaha wa dhambi[l] na urithi[m] kati ya wale waliotakaswa[n] kwa imani yao kwangu.'
19 "Kwa sababu hii, Mfalme

SURA 26
a Mdo 25:26
b Ga 1:13
c Mdo 22:3
d Mdo 23:6
Flp 3:5
e Mdo 24:15
f Mwa 3:15
Kum 18:15
2Sa 7:12
Da 9:24
Mal 3:1
g Lu 2:37
Ro 11:7
h Mdo 24:21
i 1Fa 17:22
2Fa 4:35
Ebr 11:35
j Yoh 16:2
Mdo 8:3
1Ko 15:9
Ga 1:13
1Ti 1:13
k Mdo 9:2
Mdo 9:14
l Mdo 22:19

Safu ya 2
a Mdo 9:2
Mdo 22:5
b Mdo 9:3
Mdo 22:6
c Mdo 9:4
Mdo 22:7
d Mdo 9:5
Mdo 22:8
e Eze 2:1
f Mdo 22:15
Ga 1:12
1Ti 1:12
g Mdo 22:21
Ro 11:13
h Isa 35:5
Isa 61:1
i Isa 42:7
Kol 1:13
j Isa 60:2
Yoh 8:12
2Ko 4:6
k Efe 2:2
l Lu 1:77
1Yo 3:5
m Efe 1:11
n Mdo 20:32

Agripa, mimi sikukosa ku-
tii maono hayo ya kimbingu,[a]
20 lakini kwa wale walio kati-
ka Damasko[b] kwanza na pia
kwa wale walio katika Yeru-
salemu,[c] na juu ya nchi yote
ya Yudea, na kwa mataifa[d] nili-
enda nikiuleta ujumbe kwa-
mba wao wanapaswa kutubu
na kumgeukia Mungu kwa ku-
fanya matendo yanayostahili
toba.[e] **21** Kwa sababu ya ma-
mbo haya Wayahudi walinika-
mata katika hekalu na kujaribu
kuniua.[f] **22** Hata hivyo, kwa
sababu nimeupata msaada[g] ku-
toka kwa Mungu ninaendelea
mpaka leo kutoa ushahidi kwa
wadogo na wakubwa pia, laki-
ni bila kusema lolote ila ma-
mbo ambayo Manabii[h] na vilevi-
le Musa[i] walisema yatatukia,
23 kwamba Kristo angeteseka[j]
na, akiwa wa kwanza kufufuliwa[k]
kutoka kwa wafu, angeta-
ngaza nuru[l] kwa watu hawa na
pia kwa mataifa."[m]

24 Sasa alipokuwa akisema
mambo haya kwa kujitetea, Fe-
sto akasema kwa sauti kubwa:
"Unashikwa na wazimu,[n] Paulo!
Kusoma kwingi kunakufanya
uwe na wazimu!" **25** Lakini
Paulo akasema: "Mimi sishikwi
na wazimu, ewe Mtukufu Fe-
sto, bali ninasema maneno ya
kweli na ya utimamu wa akili.
26 Kwa kweli, mfalme ambaye
ninasema naye kwa uhuru wa
kusema anajua vema juu ya ma-
mbo haya; kwa maana ninasadi-
ki kwamba hakuna hata moja
kati ya mambo haya ambalo ha-
jui, kwa maana jambo hili ha-
lijafanywa pembeni.[o] **27** Je,
wewe, Mfalme Agripa, unawaa-
mini Manabii? Ninajua una-
waamini."[p] **28** Lakini Agri-
pa akamwambia Paulo: "Kwa
muda mfupi ungenishawishi
niwe Mkristo." **29** Ndipo Pa-
ulo akasema: "Kama ingekuwa
kwa muda mfupi au kwa muda
mrefu mimi ningetaka kwa Mu-
ngu kwamba si wewe tu bali pia
wote wanaonisikia leo wapa-
te kuwa watu wa namna niliyo
mimi, ila tu bila vifungo hivi."

30 Naye mfalme akasima-
ma na pia gavana na Bernike
na watu walioketi pamo-
ja nao. **31** Lakini walipoku-
wa wakiondoka wakaanza kuo-
ngea wao kwa wao, wakisema:
"Mtu huyu hafanyi lolote li-
nalostahili kifo[a] au vifungo."
32 Zaidi ya hayo, Agripa aka-
mwambia Festo: "Mtu huyu
angaliweza kufunguliwa kama
hakuwa amekata rufani[b] kwa
Kaisari."

27 Basi kwa kuwa iliamuli-
wa tusafiri kwenda Ita-
lia,[c] walikuwa wakikabidhi Pa-
ulo na pia wafungwa fulani
wengine kwa ofisa-jeshi anaye-
itwa Yulio wa kikosi cha Au-
gusto. **2** Tukapanda ndani ya
mashua kutoka Adramitiamu,
iliyokuwa karibu kusafiri mpa-
ka kandokando ya pwani ya wi-
laya ya Asia, tukasafiri kwa ma-
shua, naye Aristarko[d] Mmake-
donia kutoka Thesalonike ali-
kuwa pamoja nasi. **3** Na siku
iliyofuata tukashuka mpaka Si-
doni, na Yulio akamtendea Pa-
ulo kwa fadhili za kibinadamu[e]
na kumruhusu aende kwa rafi-
ki zake na kutunzwa nao.[f]

4 Tulipotoka huko tukasa-
firi chini ya Kipro, kwa saba-
bu pepo zilikuwa zikitukabili;
5 nasi tukaendesha kupitia ba-
hari kuu kandokando ya Ki-
likia na Pamfilia na kuegesha

SURA 26
a Mdo 9:20
b Mdo 9:22
c Mdo 9:28
d Mdo 9:15
e Eze 18:31
Mt 3:8
2Ko 7:11
f Mdo 21:31
g 2Ko 1:10
h Isa 9:6
Yer 23:5
Yer 33:15
Eze 34:23
Mik 5:2
Mal 3:1
Lu 24:27
Lu 24:44
Ro 3:21
i Mwa 3:15
Mwa 49:10
Kum 6:4
Kum 18:18
Yoh 5:46
j Zb 22:7
Zb 22:16
Zb 35:19
Isa 50:6
Isa 53:5
k Zb 16:10
l Lu 2:32
m Zb 18:49
Isa 11:10
Isa 52:15
n 1Ko 1:23
o Yoh 18:20
p Mdo 26:3

Safu ya 2
a Mdo 23:29
Mdo 25:25
b Mdo 25:11
Mdo 25:21
Mdo 28:19

SURA 27
c Mdo 25:12
d Mdo 19:29
Mdo 20:4
Kol 4:10
e Met 19:22
Mdo 28:16
f Mdo 24:23

bandarini kule Mira katika Likia. **6** Lakini huko ofisa-jeshi akapata mashua kutoka Aleksandria[a] iliyokuwa ikisafiri kwenda Italia, naye akatupandisha chomboni. **7** Ndipo, baada ya kusafiri kwa mashua polepole kwa siku kadhaa na kufika Kinido kwa shida, kwa sababu upepo haukuturuhusu tuendelee mbele, tukasafiri chini ya Krete katika Salmone, **8** tukapita kandokando ya pwani yake kwa shida tukafika mahali fulani panapoitwa Bandari Nzuri, ambapo jiji Lasea lilikuwa karibu na hapo.

9 Kwa kuwa muda mrefu ulikuwa umepita na kufikia sasa ilikuwa hatari kusafiri kwa sababu hata kufunga kwa siku ya upatanisho[b] kulikuwa tayari kumepita, Paulo alitoa pendekezo, **10** akiwaambia: "Ninaona kwamba safari itakuwa na madhara na hasara kubwa si ya shehena na mashua tu bali pia ya nafsi zetu."[c] **11** Hata hivyo, ofisa-jeshi akawa anamsikiliza nahodha na mwenye meli badala ya mambo yaliyosemwa na Paulo. **12** Sasa kwa kuwa bandari hiyo haikufaa kukaa wakati wa majira ya baridi kali, walio wengi wakakata shauri kusafiri kutoka hapo, ili kuona kama wangeweza kwa njia fulani kufaulu kufika Feniki ili kukaa huko wakati wa majira ya baridi kali, ambayo ni bandari ya Krete inayofunguka kuelekea kaskazini-mashariki na kuelekea kusini-mashariki.

13 Zaidi ya hayo, upepo wa kusini ulipovuma kwa utulivu, walifikiri walikuwa wamefikia kusudi lao, nao wakang'oa

SURA 27

a Mdo 28:11

b Law 16:29
Law 23:27

c Mdo 27:21

Safu ya 2

a Mk 4:37

b Mdo 27:32

c Yon 1:5

d Yon 1:13

e Yon 1:9

f Mdo 27:10

nanga na kuanza kufuata pwani karibu na pwani ya Krete. **14** Hata hivyo, baada ya muda usiokuwa mrefu, upepo wenye tufani[a] unaoitwa Euroakilo ukavuma kasi juu yake. **15** Kwa kuwa mashua ilishikwa na upepo wenye nguvu nayo haikuweza kushindana na upepo huo, tukaiachilia, nao ukatuchukua. **16** Basi tukasafiri upesi chini ya kisiwa fulani kidogo kinachoitwa Kauda, na bado ilikuwa vigumu kuiongoza kikamili mashua[b] ndogo kwenye tezi. **17** Lakini baada ya kuiingiza ndani wakaanza kutumia misaada ili kuikaza mashua chini; nao wakiogopa kupanda mwamba katika Sirti, wakashusha vifaa vya kuendeshea na hivyo wakachukuliwa. **18** Lakini kwa sababu tulikuwa tukirushwarushwa kwa nguvu nyingi na tufani hiyo, siku iliyofuata tukaanza kupunguza uzito[c] wa meli; **19** na siku ya tatu, kwa mikono yao wenyewe, wakatupa ayari za mashua hiyo.

20 Basi, wakati ambapo jua wala nyota hazikuonekana kwa siku nyingi, nayo tufani[d] iliyokuwa juu yetu ikiwa si ndogo, mwishowe tukaanza kukata tumaini la kuokolewa. **21** Na baada ya kujiepusha na chakula kwa muda mrefu, Paulo akasimama katikati yao[e] na kusema: "Mlipaswa kufuata shauri langu na kutosafiri katika bahari kutoka Krete na hivyo mwepuke kupatwa na madhara na hasara hii.[f] **22** Hata hivyo, sasa ninapendekeza mchangamke, kwa maana hakuna nafsi kati yenu itakayopotea, mashua tu ndiyo itakayopotea.

23 Kwa maana usiku huu malaika[a] wa Mungu ambaye mimi ni
mali yake na ambaye mimi ninamtolea utumishi mtakatifu, ali-
simama karibu nami,[b] **24** akisema, 'Usiogope, Paulo. Utasi-
mama mbele ya Kaisari,[c] na, tazama! Mungu amekupa wale
wote wanaosafiri pamoja nawe.' **25** Kwa hiyo changamkeni;
kwa maana ninamwamini Mungu[d] kwamba itakuwa kama
vile ambavyo nimeambiwa. **26** Hata hivyo, lazima tutupwe
pwani juu ya kisiwa fulani."[e]

27 Sasa usiku wa kumi na
nne ulipofika nasi tukawa tu-
kirushwa huku na huku kati-
ka bahari ya Adria, katikati
ya usiku mabaharia wakaanza
kudhani walikuwa wakikaribia
nchi fulani. **28** Nao wakapima
kina kwa bildi na kupata
kuwa ni pima 20; kwa hiyo wa-
kaendelea mbele umbali mfupi
na wakatia bildi tena na kupata
kuwa ni pima 15. **29** Na kwa
sababu ya kuogopa kwamba tu-
ngeweza kutupwa mahali fu-
lani juu ya miamba, wakatu-
pa nanga nne kutoka kwenye
tezi na kuanza kutamani ku-
pambazuke. **30** Lakini maba-
haria walipoanza kutafuta ku-
kimbia katika mashua na ku-
shusha mashua ndogo ndani
ya bahari kwa kusingizia kuwa
walikusudia kuzishusha nanga
kutoka kwenye omo, **31** Pa-
ulo akamwambia ofisa-jeshi
na askari-jeshi: "Watu hawa
wasipobaki katika mashua,
ninyi hamwezi kuokolewa."[f]
32 Ndipo askari-jeshi wakaka-
ta kamba za mashua[g] ndogo na
kuiacha ianguke.

33 Sasa karibu na mapamba-
zuko Paulo akaanza kuwatia
moyo wote wale chakula, akise-
ma: "Leo ni siku ya kumi na nne
ambayo mmekuwa mkikesha
na kukaa bila chakula, mkiwa
hamjala chochote. **34** Kwa
hiyo ninawatia moyo mle chaku-
la, kwa ajili ya usalama wenu;
kwa maana hata unywele[a] mmo-
ja wa kichwa cha mmoja kati
yenu hautaangamia." **35** Baa-
da ya kusema jambo hilo, pia
akachukua mkate, akamshu-
kuru[b] Mungu mbele yao wote
akaumega na kuanza kula.
36 Kwa hiyo wote wakacha-
ngamka na kuanza kula cha-
kula wao wenyewe. **37** Basi,
sote pamoja, sisi nafsi tuliomo
ndani ya mashua tulikuwa
276. **38** Walipokuwa wame-
shiba chakula, wakaanza kupu-
nguza uzito[c] wa mashua kwa ku-
tupa ngano baharini.

39 Mwishowe kulipopamba-
zuka, hawakuweza kuitambua
nchi hiyo lakini walikuwa wa-
kiangalia ghuba fulani yenye
pwani, na hapo ndipo walipoa-
zimia, ikiwa wangeweza, kuipe-
leka mashua pwani.[d] **40** Kwa
hiyo, wakizikata nanga, waka-
ziacha zianguke ndani ya ba-
hari, wakati huohuo wakifu-
ngua amari za makasia ya mta-
mbo wa usukani na, baada ya
kutweka tanga la mbele kwe-
nye upepo, wakaenda pwani.
41 Walipotua juu ya fungu la
mchanga lililorundikwa na ba-
hari pande zote mbili, wakai-
endesha meli juu ya mwamba
na omo ikakwama na kukaa
bila kuondoleka, lakini tezi
likaanza kuvunjika vipande-
vipande kwa nguvu nyingi.[e]
42 Ndipo askari-jeshi wakaazi-
mia kuwaua wafungwa, ili ye-
yote asiogelee na kutoroka.

SURA 27

a Da 6:16
Mdo 5:19
Mdo 23:11
Ebr 1:14

b Ro 1:9
2Ti 1:3
Ebr 12:28

c Mdo 23:11
Mdo 25:11

d Hes 23:19
Ro 4:21
Tit 1:2

e Mdo 28:1

f Mdo 27:22

g Mdo 27:16

Safu ya 2

a 1Sa 14:45
2Sa 14:11
Mt 10:30
Lu 12:7

b Mt 15:36
Mk 8:6
Yoh 6:11
Ro 14:6
1Ti 4:4

c Yon 1:5

d Mdo 28:1

e Mdo 27:22
2Ko 11:25

43 Lakini ofisa-jeshi akataka
kumpitisha Paulo akiwa sala-
ma naye akawazuilia wasitimi-
ze kusudi lao. Naye akawaamu-
ru wale ambao wangeweza ku-
ogelea wajitupe baharini na ku-
fika kwenye nchi kavu kwanza,
44 na wale wengine wafanye
hivyo, wengine wakiwa juu ya
mbao na wengine juu ya vitu
fulani kutoka katika mashua.
Na hivyo ikawa kwamba wote
wakafika salama kwenye nchi
kavu.[a]

28 Na tulipokuwa tumefika
mahali salama, tukapa-
ta habari kwamba kisiwa hi-
cho kilikuwa kikiitwa Malta.[b]
2 Na watu hao wenye kusema
lugha ya kigeni wakatuonye-
sha fadhili[c] za kibinadamu zisi-
zo za kawaida, kwa maana wa-
liwasha moto na kutukaribisha
sote na kutupa msaada kwa sa-
babu ya mvua iliyokuwa iki-
nyesha na kwa sababu ya ba-
ridi.[d] 3 Lakini Paulo alipoku-
sanya tita la kuni na kuliweka
juu ya moto, nyoka-kipiri aka-
toka kwa sababu ya joto na ku-
jifunga kwenye mkono wake.
4 Watu hao wenye kusema lu-
gha ya kigeni walipoona huyo
kiumbe mwenye sumu akining-
'inia kwenye mkono wake,
wakaanza kuambiana: "Hakika
mtu huyu ni muuaji, na inga-
wa alifika mahali salama kuto-
ka baharini, haki yenye kudai
kisasi haikumruhusu aendelee
kuishi." 5 Hata hivyo, aka-
mkung'uta kiumbe huyo mwe-
nye sumu na kumtupa ndani
ya moto, naye hakupatwa na
dhara.[e] 6 Lakini wao walikuwa
wakitarajia atavimba kwa
sababu ya mwasho au kwa gha-
fula aanguke na kufa. Baada
ya kungojea kwa muda mre-
fu na kuona kwamba haku-
na jambo lolote baya lililompa-
ta, wakabadili maoni yao na ku-
anza kusema kwamba yeye ni
mungu.[a]
7 Sasa katika ujirani wa ma-
hali hapo mkuu wa kisiwa hi-
cho, anayeitwa Publio, alikuwa
na mashamba; naye akatukari-
bisha na kutupokea kwa hisani
kwa siku tatu. 8 Lakini ika-
wa kwamba baba ya Publio ali-
kuwa amelala akitaabishwa na
homa na ugonjwa wa kuhara
damu, na Paulo akaingia alimo-
kuwa na kusali, akaweka miko-
no[b] yake juu yake akamponya.[c]
9 Baada ya jambo hilo kutukia,
watu wale wengine kisiwani
waliokuwa na magonjwa waka-
anza pia kuja kwake na kupo-
nywa.[d] 10 Nao pia wakatupa
sisi zawadi nyingi na, tulipoku-
wa tukisafiri, wakapakia vitu
kwa ajili ya mahitaji yetu.
11 Miezi mitatu baadaye tu-
kasafiri kutoka Aleksandria[e]
kwa mashua iliyokuwa imekaa
wakati wa majira ya baridi kali
katika kisiwa hicho na yenye sa-
namu ya gubeti ya "Wana wa
Zeu." 12 Nasi tukaegesha ka-
tika bandari ya Sirakusa tu-
kakaa siku tatu, 13 mahali
ambapo kutoka hapo tulienda
tukizunguka na kufika Regia-
mu. Na siku moja baadaye upe-
po wa kusini ukazuka nasi tu-
kaingia Puteoli siku ya pili.
14 Tukawakuta akina ndugu
hapo nao wakatusihi tukae pa-
moja nao kwa siku saba; na kwa
njia hii tukaja kuelekea Roma.
15 Na kutoka huko akina ndu-
gu, waliposikia habari juu yetu,
wakaja kukutana nasi mpaka
Soko la Apio na Mikahawa Mi-

SURA 27
a Mdo 27:24

SURA 28
b Mdo 27:26
c Met 19:22 Mdo 27:3
d 2Ko 11:27
e Lu 10:19

Safu ya 2
a Mdo 14:11
b Mk 7:32 Mdo 19:11 1Ko 12:9
c Lu 4:39
d Mt 10:8
e Mdo 27:6

tatu na, alipowaona, Paulo aka-
mshukuru Mungu na kujipa
moyo.[a] **16** Mwishowe, tulipoi-
ngia Roma, Paulo akaruhusiwa[b]
kukaa akiwa peke yake pamoja
na askari-jeshi mwenye kumli-
nda.

17 Hata hivyo, siku tatu ba-
adaye akawaita pamoja wale
waliokuwa wakuu wa Wayahu-
di. Walipokuwa wamekusanyi-
ka, akaanza kuwaambia: "Wa-
naume, akina ndugu, ijapoku-
wa sikuwa nimefanya jambo
lolote kinyume cha watu au de-
sturi za mababu zetu,[c] nili-
tolewa nikiwa mfungwa Ye-
rusalemu na kutiwa miko-
noni mwa Waroma.[d] **18** Na
hawa, baada ya kufanya uchu-
nguzi,[e] walitaka kunifungua,[f]
kwa kuwa hakukuwa na sa-
babu yoyote kwangu ya kuua-
wa.[g] **19** Lakini Wayahudi wa-
lipoendelea kusema vibaya juu
ya jambo hilo, nililazimika ku-
kata rufani[h] kwa Kaisari, la-
kini si kana kwamba nilikuwa
na jambo lolote la kushtaki tai-
fa langu. **20** Kwa kweli kwa
sababu hii nilisihi niwaone na
kusema nanyi, kwa maana ni-
mefungwa mnyororo[i] huu kwa
sababu ya tumaini[j] la Israeli."
21 Wakamwambia: "Wala sisi
hatujapokea barua zinazoku-
husu wewe kutoka Yudea, wala
hakuna yeyote wa akina ndugu
ambaye amefika aliyetujulisha
au kusema jambo lolote baya
juu yako. **22** Lakini tunaona
inafaa kusikia maoni yako ku-
toka kwako, kwa maana kwe-
li kwa habari ya madhehebu[k]
hii tunajua kwamba kila maha-
li huwa inasemwa vibaya."[l]

23 Basi wakapanga siku fu-
lani ya kuwa pamoja naye, nao
wakaja kwake wakiwa hesa-
bu kubwa zaidi katika makao
yake. Naye akawaeleza jambo
hilo kwa kutoa ushahidi kami-
li kuhusiana na ufalme wa Mu-
ngu[a] na kwa kutumia ushawi-
shi kwao kuhusu Yesu kuto-
ka katika sheria ya Musa[b] na
pia Manabii,[c] tangu asubuhi
mpaka jioni. **24** Na wengine
wakaanza kuamini[d] mambo ya-
liyosemwa; wengine hawakua-
mini.[e] **25** Kwa hiyo, kwa sa-
babu walikosa kukubaliana,
wakaanza kuondoka, huku Pa-
ulo akieleza jambo hili moja:

"Roho takatifu kwa kufaa ili-
sema kupitia Isaya nabii kwa
mababu zenu, **26** ikisema,
'Nenda kwa watu hawa na ku-
sema: "Kwa kusikia, mtasikia
lakini msielewe kamwe; na, ku-
tazama, mtatazama, lakini msi-
one kamwe.[f] **27** Kwa maana
moyo wa watu hawa umekuwa
mgumu, na kwa masikio yao
wamesikia bila kuitikia, nao
wamefunga macho yao; ili wasi-
one kamwe kwa macho yao na
kusikia kwa masikio yao na ku-
elewa kwa moyo wao na ku-
geuka, nami niwaponye."'[g]
28 Kwa hiyo jueni kwamba
njia hii ambayo Mungu anai-
tumia kuokoa, imepelekwa
nje kwa mataifa;[h] wao hakika
wataisikiliza."[i] **29** ——

30 Kwa hiyo akakaa miaka
miwili kamili katika nyumba
yake mwenyewe ya kukodi-
wa,[j] naye akawa akiwakaribi-
sha kwa fadhili wale wote wa-
lioingia ndani kwake, **31** aki-
wahubiria ufalme wa Mungu na
kufundisha mambo yanayohu-
su Bwana Yesu Kristo kwa uhu-
ru wa kusema[k] ulio mkubwa za-
idi, bila kizuizi.

SURA 28

a 2Ko 1:4
b Mdo 24:23
c Mdo 24:12
Mdo 25:8
d Mdo 21:33
e Mdo 24:10
f Mdo 26:32
g Mdo 23:9
Mdo 23:29
Mdo 25:25
Mdo 26:31
h Mdo 25:11
Mdo 26:32
i Efe 6:20
2Ti 1:16
j Mdo 23:6
Mdo 26:6
Tit 2:13
k Mdo 24:14
l Lu 2:34
Yoh 15:19

Safu ya 2

a Mdo 17:2
Mdo 26:22
b Mwa 3:15
Mwa 22:18
Mwa 49:10
Kum 18:18
Kum 32:43
Yoh 5:46
c Isa 9:6
Isa 11:10
Isa 52:15
Yer 23:5
Mik 5:2
Zek 13:7
Mal 3:1
Lu 24:44
d Mdo 17:4
e Mdo 14:4
2Th 3:2
f Isa 6:9
Yer 5:31
Eze 12:2
Ro 11:8
g Isa 6:10
h Lu 3:6
Mdo 13:46
Mdo 22:21
Ro 11:11
i Zb 67:2
Zb 98:3
Isa 11:10
j Mdo 28:16
k Mdo 26:26
Efe 6:19

WAROMA

1 Paulo, mtumwa[a] wa Yesu
Kristo aliyeitwa[b] kuwa mtu-
me,[c] aliyetengwa kwa ajili ya ha-
bari njema ya Mungu,[d] **2** aliyo-
ahidi kimbele kupitia manabii[e]
wake katika Maandiko matakatifu, **3** kuhusu Mwana wake, aliyetokana na uzao wa Daudi[f] kulingana na mwili,[g] **4** lakini ambaye kwa nguvu[h] alitangazwa kuwa Mwana wa Mungu[i] kulingana na roho[j] ya utakatifu kwa njia ya ufufuo kutoka kwa wafu[k]—ndiyo, Yesu Kristo Bwana wetu, **5** ambaye kupitia yeye tulipokea fadhili zisizostahiliwa[l] na utume[m] ili kuwe na utii wa imani kati ya mataifa[n] yote kuhusu jina lake, **6** mataifa ambayo kati yake ninyi pia ni wale walioitwa kuwa wa Yesu Kristo— **7** kwa wale wote walio katika Roma wakiwa wapendwa wa Mungu, walioitwa[o] wawe watakatifu:[p]

Na muwe na fadhili zisizostahiliwa na amani[q] kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.[r]

8 Kwanza kabisa, namshukuru[s] Mungu wangu kupitia Yesu Kristo kuhusu ninyi nyote, kwa sababu imani yenu inazungumzwa[t] kotekote ulimwenguni. **9** Kwa maana Mungu, ambaye ninamtolea utumishi mtakatifu kwa roho yangu kuhusiana na ile habari njema juu ya Mwana wake, ni shahidi[u] wangu wa jinsi ninavyowataja sikuzote katika sala zangu bila kuacha,[v] **10** nikiomba kwamba ikiwa kwa vyovyote inawezekana sasa mwishowe nipate kufanikiwa katika mapenzi[a] ya Mungu ili nije kwenu. **11** Kwa maana ninatamani kuwaona ninyi,[b] ili niwape sehemu ya zawadi ya kiroho[c] kusudi mfanywe imara; **12** au, badala ya hivyo, kwamba kuwe na ubadilishanaji wa kitia-moyo kati yenu,[d] kila mmoja kupitia imani ya mwingine,[e] yenu na yangu pia.

13 Lakini, akina ndugu,[f] sitaki mkose kujua kwamba mara nyingi nilikusudia kuja kwenu[g] ili niweze kujipatia matunda fulani[h] kati yenu pia kama vile ilivyo kati ya mataifa mengine, lakini nimezuiwa mpaka sasa. **14** Mimi nina deni kwa Wagiriki na kwa Wabaribari pia, kwa wenye hekima[i] na kwa wasio na akili pia: **15** kwa hiyo nina hamu ya kuitangaza habari njema[j] kwenu pia mlio huko Roma.[k] **16** Kwa maana siionei aibu[l] habari njema; kwa kweli, hiyo ni nguvu za Mungu[m] kwa ajili ya wokovu kwa kila mtu aliye na imani,[n] kwa Myahudi kwanza[o] na pia kwa Mgiriki;[p] **17** kwa maana katika hiyo uadilifu[q] wa Mungu unafunuliwa kwa sababu ya imani[r] na kuelekea imani, kama vile ilivyoandikwa: "Lakini mwadilifu—ataishi kwa njia ya imani."[s]

18 Kwa maana ghadhabu[t] ya Mungu inafunuliwa kutoka mbinguni juu ya watu wote wasiomwogopa Mungu na wasio

SURA 1
a Ga 1:10
b Mdo 9:15
Ga 1:15
c 1Ko 15:9
d Ga 3:8
e Hes 12:6
Lu 1:70
Tit 1:2
f 2Sa 7:12
Lu 1:32
2Ti 2:8
g Yoh 1:14
Ga 4:4
h 2Ko 13:4
i Zb 2:7
Ebr 1:5
j Lu 11:13
Efe 1:13
1Ti 3:16
k Zb 16:10
Mdo 3:15
Mdo 13:33
l Yoh 1:16
Efe 3:8
m 1Ti 2:7
2Ti 1:11
n Mdo 15:14
Ga 2:7
o Flp 3:14
1Th 2:12
Ebr 3:1
p 1Ko 1:2
q Efe 6:23
r 1Ko 1:3
Ga 1:3
s Flp 1:3
t Ro 16:19
1Th 1:8
u 2Ko 1:23
Flp 1:8
v 1Th 3:10
2Ti 1:3

Safu ya 2
a Mdo 18:21
Ro 15:32
Yak 4:15
b Flp 1:8
Flp 4:1
1Th 2:17
c Ro 15:29
d Flp 2:1
1Th 5:11
Ebr 10:25
e Ga 6:10
1Ti 4:10
1Pe 1:7
f Mk 3:35
g Ro 15:23
h Yoh 15:16
Flp 4:17
i 1Ko 3:18
j Mk 13:10
k Mdo 19:21
l Zb 119:46
Mk 8:38
2Ti 1:8
m 1Ko 1:18
n Ebr 11:6
o Mdo 3:26
p Mdo 18:6
q Ro 3:21
r Yoh 3:36
Flp 3:9

s Hab 2:4; Ga 3:11; Ebr 10:38; t Ro 2:5; Efe 5:6.

waadilifu[a] ambao wanaikandamiza kweli[b] katika njia isiyo ya
uadilifu,[c] **19** kwa sababu yale
yanayoweza kujulikana juu ya
Mungu yamefunuliwa katika-
ti yao,[d] kwa maana Mungu ali-
yafunua kwao.[e] **20** Kwa maa-
na sifa zake ambazo hazione-
kani,[f] zinaonekana waziwazi ta-
ngu kuumbwa kwa ulimwengu
na kuendelea,[g] kwa sababu zi-
naeleweka kwa vitu vilivyo-
fanywa,[h] yaani, nguvu zake za
milele[i] na Uungu,[j] hivi kwamba
hawana sababu ya kujitetea.[k]
21 Kwa sababu, ijapokuwa wa-
limjua Mungu, hawakumtuku-
za yeye kuwa Mungu wala ha-
wakumshukuru,[l] bali wakawa
wajinga[m] katika kufikiri kwao
na moyo wao usio na ufahamu
ukaingiwa na giza.[n] **22** Ijapo-
kuwa walisisitiza kuwa ni we-
nye hekima, wakawa wapumba-
vu[o] **23** na kuugeuza utuku-
fu[p] wa Mungu asiye na uharibi-
fu kuwa kitu kama sanamu[q] ya
mwanadamu aliye na uharibifu
na ya ndege na viumbe vyenye
miguu minne na vitu vinavyo-
tambaa.[r]

24 Kwa hiyo, kwa kupatana
na tamaa za mioyo yao, Mungu
aliwaacha katika uchafu,[s] ili
miili[t] yao ivunjiwe heshima kati
yao,[u] **25** yaani, wale walioiba-
dili kweli[v] ya Mungu kwa aji-
li ya uwongo[w] nao wakauhe-
shimu mno uumbaji na kuu-
tolea utumishi mtakatifu bada-
la ya kumtolea Yeye aliyeumba,
anayebarikiwa milele. Amina.
26 Ndiyo sababu Mungu aliwa-
acha katika hamu za ngono ye-
nye kufedhehesha,[x] kwa maa-
na wanawake wao walibadili
matumizi yao wenyewe ya asili
kuwa yale yaliyo kinyume cha

SURA 1

a Ayu 24:13
b Ro 1:25
c Yoh 8:44
d Mdo 14:17
e Zb 19:1
f 1Ti 1:17
Ebr 11:27
g Isa 40:21
h Isa 40:26
Ufu 4:11
i Yer 10:12
2Pe 1:3
j Zb 103:19
Yer 10:10
Ufu 15:3
k Mdo 17:27
Ro 3:2
l Kum 4:8
Zb 50:23
Zb 147:19
m Mt 23:28
Tit 1:14
n Mwa 6:5
Mt 9:4
Mt 13:15
Lu 5:22
o Mt 23:17
2Pe 2:19
p Yer 2:11
Ho 4:7
Mdo 17:29
q Kum 4:16
Zb 106:20
Mdo 14:15
r Kum 4:17
Eze 8:10
s Zb 81:12
Mdo 7:42
2Ko 12:21
Ga 5:19
t 1Ko 6:18
u Law 18:22
Efe 5:12
v Mt 4:10
Yoh 8:32
Ro 2:8
w Zb 10:4
Zb 14:1
Mal 3:14
Yoh 8:44
2Th 2:11
2Ti 4:4
x 1Th 4:5

Safu ya 2

a Law 18:23
Yud 7
b Law 18:22
c Mwa 19:5
Law 20:13
1Ko 6:9
d Ro 6:21
Efe 5:4
e Kum 7:15
Ga 6:7
2Pe 2:13
f 2Pe 2:19
Yud 10
g Ebr 10:26
h Ro 11:7
2Ko 3:14
i Ga 5:19
2Ti 3:2
j 1Pe 4:3
k Mk 7:22
l Kum 5:21
2Pe 2:14
m 1Pe 2:16
n Tit 3:3
o Yak 4:2
1Yo 3:15
p Ga 5:20
q 1Th 2:3
1Pe 2:1

asili;[a] **27** na vivyo hivyo pia
hata wanaume waliacha matu-
mizi ya asili ya mwanamke[b]
na kuwakiana tamaa kali katika
uchu wao kuelekeana wao we-
nyewe, wanaume kwa wanau-
me,[c] wakitenda mambo macha-
fu[d] na kupokea ndani yao we-
nyewe malipo kamili,[e] yaliyosta-
hili kosa lao.[f]

28 Na kama vile ambavyo ha-
wakukubali kumjua Mungu ka-
tika ujuzi sahihi,[g] Mungu ali-
waacha katika hali ya akili ili-
yokataliwa,[h] ili wafanye mambo
yasiyofaa,[i] **29** wakiwa wame-
jawa na ukosefu wote wa uadi-
lifu,[j] uovu,[k] tamaa,[l] ubaya,[m] wa-
kiwa wamejaa wivu,[n] uuaji,[o] mi-
zozo,[p] udanganyifu,[q] mwelekeo
wenye madhara,[r] wakiwa wano-
ng'onezaji,[s] **30** wasengenya-
ji,[t] wenye kumchukia Mungu,
wenye dharau,[u] wenye majivu-
no,[v] wenye kujidai,[w] wenye ku-
tunga mambo mabaya,[x] wasio-
tii wazazi,[y] **31** wasio na uele-
waji,[z] waongo kwa mapatano,[a]
wasio na upendo wa asili,[b] wa-
sio na rehema.[c] **32** Ijapokuwa
hawa wanajua vema kabisa amri
ya uadilifu ya Mungu,[d] kwamba
wale wanaozoea kufanya ma-
mbo ya namna hiyo wanastahili
kifo,[e] wao wanaendelea kuyafa-
nya na vilevile hukubaliana[f] na
wale wanaozoea kuyafanya.

2 Kwa hiyo wewe huna saba-
bu ya kujitetea, Ee mwa-
nadamu,[g] hata uwe nani, ukihu-
kumu;[h] kwa maana katika ja-
mbo lile ambalo unamhukumu
mwingine, unajihukumu mwe-
nyewe kuwa una hatia, kwa

r Efe 4:31; 1Ti 5:13; s Met 11:13; t 1Pe 2:1; u Zb 10:13; v 2Ti 3:2; w Met 21:24; x Zb 140:2; y Kum 21:18; z Zb 32:9; Ro 1:21; a 1Ti 1:10; b Kum 28:54; 2Ti 3:3; c Yak 2:13; d Kum 4:8; e Kum 22:21; 2Th 2:12; Ufu 21:8; f Zb 50:18; Ho 7:3; **SURA 2** g Ro 2:9; Ro 9:20; h Ro 14:10; Yak 4:11.

sababu wewe unayehukumu[a]
una mazoea ya kufanya mambo
hayo hayo.[b] **2** Sasa tunajua
kwamba, kupatana na kweli,[c]
hukumu ya Mungu iko juu ya
wale walio na mazoea ya kufa-
nya mambo ya namna hiyo.
3 Lakini je, wewe unafikiri,
Ee mwanadamu,[d] kwamba uta-
ponyoka hukumu ya Mungu wa-
kati unapohukumu wale walio
na mazoea ya kufanya mambo
ya namna hiyo na bado wewe
unayafanya?[e] **4** Au je, wewe
unadharau utajiri wa fadhi-
li[f] zake na uvumilivu wenye su-
bira[g] na ustahimilivu,[h] kwa sa-
babu hujui kwamba sifa ya fa-
dhili za Mungu inajaribu ku-
kuongoza wewe kwenye toba?[i]
5 Lakini kulingana na ugumu[j]
wako na moyo wako usiotu-
bu[k] unajiwekea mwenyewe aki-
ba ya ghadhabu[l] katika siku
ya ghadhabu[m] na ya kufunuliwa[n]
kwa hukumu ya uadilifu
ya Mungu.[o] **6** Naye atamlipa
kila mmoja kulingana na ma-
tendo yake:[p] **7** uzima wa mi-
lele kwa wale wanaotafuta utu-
kufu na heshima na kutoharibi-
ka,[q] kwa uvumilivu katika kazi
iliyo njema; **8** hata hivyo, kwa
wale wenye ugomvi[r] na wale wa-
sioitii kweli[s] bali hutii ukosefu
wa uadilifu kutakuwa na gha-
dhabu na hasira,[t] **9** dhiki na
taabu, juu ya nafsi ya kila mtu
anayefanya mabaya, ya Mya-
hudi[u] kwanza na pia ya Mgiri-
ki;[v] **10** bali utukufu na he-
shima na amani kwa kila mtu
anayefanya mema,[w] kwa Mya-
hudi kwanza[x] na pia kwa Mgi-
riki.[y] **11** Kwa maana hakuna
ubaguzi kwa Mungu.[z]
12 Kwa mfano, wale wote
waliofanya dhambi bila she-
ria wataangamia pia bila she-
ria;[a] bali wale wote waliofanya
dhambi chini ya sheria[b] watahu-
kumiwa kwa sheria.[c] **13** Kwa
maana wasikiaji wa sheria sio
walio waadilifu mbele za Mu-
ngu, bali watendaji[d] wa sheria
watatangazwa kuwa waadilifu.[e]
14 Kwa maana wakati watu wa
mataifa[f] wasio na sheria[g] wa-
napofanya kwa asili mambo ya
sheria,[h] watu hawa, ijapoku-
wa hawana sheria, wao ni she-
ria kwao wenyewe. **15** Wao
ndio wanaoonyesha kuwa yali-
yomo katika sheria yameandi-
kwa ndani ya mioyo yao,[i] huku
dhamiri[j] yao ikiwatolea ushahi-
di na, katikati ya fikira zao we-
nyewe, wanashtakiwa[k] au hata
kutetewa. **16** Hili litakuwa
katika siku Mungu anapohuku-
mu kupitia Kristo Yesu[l] mambo
ya siri[m] ya wanadamu,[n] kuliga-
na na habari njema ninayoita-
ngaza.[o]
17 Sasa, ikiwa wewe ni Mya-
hudi kwa jina[p] na unategemea
sheria[q] na kujivunia Mungu,[r]
18 nawe unajua mapenzi yake[s]
na kuyakubali mambo yaliyo
bora kabisa kwa sababu una-
fundishwa kwa mdomo kutoka-
na na Sheria;[t] **19** nawe ume-
sadikishwa kwamba wewe ni ki-
ongozi wa walio vipofu,[u] nuru
kwa wale walio katika giza,[v]
20 mrekebishaji wa wale wa-
sio na akili,[w] mwalimu wa wa-
toto wachanga,[x] na ukiwa na
picha[y] ya ujuzi na ya ile kwe-
li[z] katika Sheria— **21** hata hi-
vyo, je, wewe unayemfundisha
mtu mwingine, hujifundishi
mwenyewe?[a] Wewe, unayehu-

SURA 2

a Mt 7:5
b Ro 2:21
c Isa 11:3
2Th 1:6
d Ro 2:17
e Mt 23:33
Mk 12:40
1Ti 5:24
f Zb 86:5
Ro 11:22
Efe 1:7
g Ro 3:25
h Kut 34:6
Isa 30:18
i 2Ti 2:25
2Pe 3:9
j Kum 9:6
Eze 3:7
k 1Sa 6:6
l Kum 32:35
Met 28:14
m Ufu 6:17
n 2Th 1:7
o Mdo 17:31
Ufu 11:18
p Ayu 34:11
Zb 62:12
Met 24:12
Eze 18:30
Mt 16:27
Yoh 5:29
q 1Ko 15:53
Ufu 20:6
r Flp 2:3
s Mt 4:10
Yoh 8:44
Ga 5:7
t Isa 3:11
Ro 1:18
Kol 3:6
Ebr 10:27
u Amo 3:2
v 2Th 1:6
w Ga 5:22
x Yoh 4:22
Mdo 13:46
y Mdo 15:14
z Kum 10:17
2Nya 19:7
Mdo 10:34

Safu ya 2

a Efe 2:12
Kol 2:13
b Ro 3:19
c Ro 7:9
d Kum 30:14
Eze 20:11
Yak 1:22
e Mdo 13:39
Ga 3:11
f Kum 26:19
g Zb 147:20
h Mdo 10:2
i Mdo 10:4
j 1Ko 8:7
1Pe 3:16
k Mwa 4:13
l Yoh 5:22
Mdo 10:42
Mdo 17:31
m Lu 8:17
1Ti 5:25
n 1Pe 4:5
o 2Ko 5:10
1Pe 4:6
p Ro 9:6
q Mik 3:11
Mt 23:23
Lu 11:46
r Isa 45:25
Yoh 8:41
s Kum 4:8
Zb 143:10
t Ro 3:2

u Isa 42:7; Mt 15:14; Mt 23:16; v Isa 49:6; w 2Fa 5:11; x Isa 42:6; Mt 15:26; y Kut 25:9; Mdo 7:44; Ebr 8:5; Ebr 10:1; z Ro 1:25; Kol 2:17; a Mt 23:3.

biri "Usiibe,"[a] je, wewe huiba?[b]
22 Wewe, unayesema "Usifanye
uzinzi," je, wewe hufanya uzi-
nzi?[c] Wewe, unayechukizwa na
sanamu, je, wewe huiba[d] katika
mahekalu? **23** Wewe, unayeji-
vunia sheria, je, kwa kuivunja
Sheria[e] unamvunjia Mungu he-
shima? **24** Kwa maana "jina la
Mungu linafanyiwa makufuru
katikati ya mataifa kwa sababu
yenu";[f] kama ilivyoandikwa.
25 Kwa kweli, kutahiriwa[g]
kuna faida ikiwa tu unazoea
kuifuata sheria;[h] lakini ikiwa
wewe ni mvunjaji wa sheria,[i] ku-
tahiriwa kwako kumekuwa ku-
totahiriwa.[j] **26** Kwa hiyo, iki-
wa mtu asiyetahiriwa[k] huya-
shika matakwa[l] ya uadilifu ya
Sheria, kutotahiriwa kwake
kutahesabiwa kuwa kutahiri-
wa, sivyo?[m] **27** Na mtu asiye-
tahiriwa aliye hivyo kwa asi-
li, kwa kuishika Sheria, ataku-
hukumu[n] wewe ambaye ukiwa
na sheria zilizoandikwa na uki-
wa na hali ya kutahiriwa una-
ivunja sheria. **28** Kwa maana
yeye si Myahudi aliye hivyo kwa
nje,[o] wala kutahiriwa si kule
ambako ni kwa nje juu ya mwi-
li.[p] **29** Bali yeye ni Myahudi
aliye hivyo kwa ndani,[q] na kuta-
hiriwa kwake ni kule kwa moyo[r]
kupitia roho, wala si kupitia
sheria zilizoandikwa.[s] Sifa[t] ya
mtu huyo hutoka, si kwa wana-
damu, bali kwa Mungu.[u]

3 Basi, Myahudi[v] ana ubora
gani, au ni nini faida ya ku-
tahiriwa?[w] **2** Ni nyingi katika
kila njia. Kwanza kabisa, kwa
sababu wao walikabidhiwa ma-
neno matakatifu ya Mungu.[x]
3 Basi, hali ikoje? Ikiwa wengi-
ne hawakuonyesha imani,[y] je,
ukosefu wao wa imani labda uta-

SURA 2
a Kut 20:15
Yos 7:11
b Mk 12:40
c Kum 5:18
1Ko 6:9
d Mal 3:8
e Zb 78:10
f Isa 52:5
Eze 36:20
g Mwa 17:10
h Ga 5:3
i 1Ko 7:19
j Yer 9:25
Ga 5:6
k Efe 2:11
l Mdo 10:2
m Ro 4:10
n Mt 12:41
o Yoh 8:39
Ufu 2:9
p Yoh 7:24
1Ko 7:19
q Ro 9:6
r Kum 10:16
Kum 30:6
Yer 4:4
Mdo 7:51
Flp 3:3
s Ro 7:6
t 1Ko 4:5
u Yoh 5:44

SURA 3
v Ro 9:4
w Yoh 4:22
x Kum 4:8
Zb 147:19
Mdo 7:38
y 2Th 3:2
Ebr 4:2

Safu ya 2
a 2Ti 2:13
b Hes 23:19
Isa 55:11
c 1Fa 18:39
Yoh 3:33
Yoh 8:26
d Zb 116:11
Yer 8:9
Yer 9:5
e Zb 51:4
Lu 7:29
f Ro 1:17
Flp 3:9
g Mwa 18:25
h Ga 3:15
i Zb 9:8
Zb 96:13
Zb 98:9
Mdo 17:31
j 1Ti 2:7
k Mdo 24:20
l Mt 28:15
m Ro 6:1
n Mt 23:38
o Ebr 2:2
p Ro 11:17
q Ro 3:23
Ga 3:22
r Zb 14:1
Met 20:9
Mhu 7:20
s Zb 14:2
Zb 53:2
t Zb 14:3
Zb 53:3

fanya uaminifu[a] wa Mungu usi-
we na matokeo?[b] **4** Hilo lisite-
ndeke kamwe! Bali Mungu na
aonekane kuwa wa kweli,[c] inga-
wa kila mwanadamu aonekane
kuwa mwongo,[d] kama ilivyoa-
ndikwa: "Ili uonekane kuwa
mwadilifu katika maneno yako
na ushinde wakati unapohuku-
miwa."[e] **5** Hata hivyo, ikiwa
ukosefu wetu wa uadilifu una-
tokeza wazi uadilifu[f] wa Mu-
ngu, tutasema nini? Je, Mu-
ngu hukosa haki[g] anapofungu-
lia ghadhabu yake? (Ninasema
kama mwanadamu[h] anavyose-
ma.) **6** Hilo lisitendeke ka-
mwe! Ikiwa hivyo, Mungu atau-
hukumu ulimwengu jinsi gani?[i]
7 Lakini ikiwa kwa sababu
ya uwongo wangu kweli ya Mu-
ngu[j] imefanywa ionekane wazi
zaidi kwa utukufu wake, kwa
nini bado mimi pia ninahuku-
miwa kuwa mtenda-dhambi?[k]
8 Na kwa nini isisemwe, kama
tunavyoshtakiwa kwa uwongo[l]
na kama watu fulani wanavyo-
sema kuwa sisi husema: "Na tu-
fanye mambo mabaya ili mambo
mema yaje"?[m] Hukumu[n] juu ya
watu hao inapatana na haki.[o]
9 Tuseme nini basi? Je, sisi
tuna hali bora?[p] Sivyo hata ki-
dogo! Kwa maana hapo juu tu-
mefanya shtaka kwamba Wa-
yahudi na vilevile Wagiriki
wote wako chini ya dhambi;[q]
10 kama ilivyoandikwa: "Haku-
na mwanadamu mwadilifu, ha-
kuna hata mmoja;[r] **11** haku-
na yeyote aliye na ufahamu wo-
wote, hakuna yeyote anayemta-
futa Mungu.[s] **12** Watu wote
wamepotoka, wote pamoja wa-
mekuwa wasiofaa kitu; hakuna
yeyote anayetenda fadhili, ha-
kuna hata mmoja."[t] **13** "Koo

yao ni kaburi lililo wazi, wa-
medanganya kwa ndimi zao."[a]
"Sumu ya nyoka iko nyuma
ya midomo yao."[b] **14** "Na ki-
nywa chao kimejaa kulaani na
maneno machungu."[c] **15** "Mi-
guu yao inaharakisha kwenda
kumwaga damu."[d] **16** "Uhari-
bifu na taabu zimo katika njia
zao,[e] **17** nao hawajaijua njia
ya amani."[f] **18** "Hakuna ku-
mwogopa Mungu mbele ya ma-
cho yao."[g]

19 Sasa tunajua kwamba ma-
mbo yote ambayo Sheria[h] inase-
ma, inawaambia wale walio chi-
ni ya Sheria, ili kila kinywa kizi-
bwe[i] na ulimwengu wote ustahi-
li[j] adhabu kutoka kwa Mungu.[k]
20 Kwa hiyo hakuna mwili wo-
wote utakaotangazwa kuwa
mwadilifu[l] kutokana na mate-
ndo ya sheria[m] mbele zake, kwa
maana ujuzi sahihi juu ya dha-
mbi ni kwa njia ya sheria.[n]

21 Lakini sasa uadilifu[o] wa
Mungu umefunuliwa bila she-
ria, kama unavyotolewa usha-
hidi[p] na Sheria[q] na Manabii;[r]
22 ndiyo, uadilifu wa Mungu
kupitia imani katika Yesu Kri-
sto,[s] kwa ajili ya wote walio
na imani.[t] Kwa maana haku-
na tofauti.[u] **23** Kwa maana
wote wamefanya dhambi[v] na
kupungukiwa na utukufu wa
Mungu,[w] **24** nayo ni zawadi
ya bure[x] kwamba wanatanga-
zwa kuwa waadilifu kwa fa-
dhili zake zisizostahiliwa[y] ku-
pitia kuachiliwa huru kwa
njia ya fidia[z] ambayo Kristo
Yesu alilipa. **25** Mungu ali-
mweka kuwa toleo la kupatani-
sha[a] kupitia imani katika damu[b]
yake. Ilikuwa hivyo ili kuonye-
sha wazi uadilifu wake mwe-
nyewe, kwa sababu alikuwa
akizisamehe dhambi[a] zilizoto-
kea wakati uliopita wakati Mu-
ngu alipokuwa akivumilia kwa
subira;[b] **26** ili kuonyesha wazi
uadilifu[c] wake mwenyewe kati-
ka majira haya yaliyopo, ili awe
mwadilifu hata anapomtangaza
kuwa mwadilifu[d] mtu aliye na
imani katika Yesu.

27 Basi, kujisifu[e] kuko wapi?
Kumefungiwa nje. Kupitia she-
ria[f] gani? Ile ya matendo?[g] Ha-
pana, bali kupitia sheria ya
imani.[h] **28** Kwa maana tu-
naamua kwamba mtu hutanga-
zwa kuwa mwadilifu kwa imani
bila matendo ya sheria.[i] **29** Au
je, yeye ni Mungu wa Wayahudi
peke yao?[j] Je, yeye si wa watu
wa mataifa pia?[k] Ndiyo, wa watu
wa mataifa pia,[l] **30** ikiwa kwa
kweli Mungu ni mmoja,[m] ata-
kayewatangaza watu waliotahi-
riwa[n] kuwa waadilifu kutoka-
na na imani na watu wasiotahi-
riwa[o] kuwa waadilifu kwa njia
ya imani yao. **31** Basi, je, tu-
naifuta sheria kupitia imani
yetu?[p] Hilo lisitendeke kamwe!
Kinyume cha hilo, sisi tunaiima-
risha sheria.[q]

4 Kwa kuwa iko hivyo, tuta-
sema nini juu ya Abrahamu
babu[r] yetu kulingana na mwili?
2 Kwa mfano, kama Abraha-
mu angetangazwa kuwa mwa-
dilifu kwa sababu ya matendo,[s]
angekuwa na sababu ya kuji-
sifu; lakini si mbele za Mungu.
3 Kwa maana andiko linase-
ma nini? "Abrahamu alionyesha
imani katika Yehova, na hilo li-
kahesabiwa kwake kuwa ni ua-
dilifu."[t] **4** Basi kwa mtu ana-
yefanya kazi,[u] malipo yanahesa-

SURA 3
a Zb 5:9; Zb 52:2
b Zb 58:4; Zb 140:3; Mt 12:34; Yak 3:8
c Zb 10:7; Yak 3:9
d Met 1:16; Isa 59:7
e Isa 59:7
f Isa 59:8
g Mwa 20:11; Zb 36:1; Zb 112:1; Met 16:6
h Ga 3:24
i Zb 63:11
j Ro 5:13
k Ro 2:12; Ga 3:10
l Mdo 13:39; Ga 3:11
m Ro 7:9
n Ro 7:13; Ga 3:19
o Kum 32:4; Ro 1:17
p Ebr 11:4
q Hes 21:9; Kum 18:18
r Isa 53:11; Yer 31:34; Da 9:24
s Yoh 1:17
t Isa 59:20
u Ga 3:28
v Mhu 7:20; Ro 3:9
w Mwa 1:31; Isa 64:6
x Ro 5:17; Ro 6:23; Efe 1:7
y Efe 2:8
z Mt 20:28; 1Ko 1:30; 1Ti 2:6; 1Pe 2:24
a Isa 53:11; 2Ko 5:19; 1Yo 2:2; 1Yo 4:10
b Law 17:11; Mdo 13:39; Efe 1:7

Safu ya 2
a Mdo 13:38
b Mdo 17:30; Ro 2:4
c Zb 89:14; Ro 5:18
d Ro 8:33; 1Ko 1:30; 1Yo 1:9
e 1Ko 1:29
f Mdo 13:39
g Efe 2:9
h Yer 31:33; Ro 1:17; Ro 8:2
i Mdo 13:39; Ga 2:16; Yak 2:24
j Mdo 17:27
k Mdo 10:4
l Isa 54:5; Ro 10:12; Ga 3:14
m Kum 6:4; Mk 12:29; 1Ko 8:6; Efe 4:6; 1Ti 2:5

n 1Ko 7:18; o Ga 3:8; p Mt 5:17; q Ro 8:4; Ro 13:10; **SURA 4** r Isa 51:2; Yoh 8:39; s Mwa 12:4; Kum 6:25; t Mwa 15:6; Ga 3:6; Yak 2:23; u Ro 9:32.

biwa kuwa ni deni,[a] wala si
kuwa ni fadhili zisizostahiliwa.[b]
5 Kwa upande mwingine, kwa
mtu asiyefanya kazi bali anay-
eweka imani[c] katika yeye
anayemtangaza kuwa mwadili-
fu yule asiyemwogopa Mungu,
imani yake inahesabiwa kuwa
ni uadilifu.[d] **6** Kama vile Dau-
di pia anavyosema juu ya fu-
raha ya mtu ambaye Mungu
humhesabia kuwa ni uadili-
fu bila matendo: **7** "Wenye fu-
raha ni wale ambao matendo
yao ya kuasi sheria yamesame-
hewa[e] na ambao dhambi zao zi-
mefunikwa;[f] **8** mwenye fura-
ha ni mtu ambaye Yehova hata-
hesabu dhambi yake kamwe."[g]

9 Basi, je, furaha hiyo huja
juu ya watu waliotahiriwa au
pia juu ya watu wasiotahiri-
wa?[h] Kwa maana tunasema:
"Imani yake ilihesabiwa kwa
Abrahamu kuwa ni uadilifu."[i]
10 Basi, ilihesabiwa chini ya
hali gani? Alipokuwa katika
kutahiriwa au katika kutota-
hiriwa?[j] Si katika kutahiri-
wa, bali katika kutotahiriwa.
11 Naye alipokea ishara,[k] ya-
ani, kutahiriwa, kuwa muhuri
wa uadilifu kwa imani aliyoku-
wa nayo alipokuwa katika hali
yake ya kutotahiriwa, ili yeye
awe baba[l] ya wale wote walio na
imani[m] wakiwa katika kutotahi-
riwa, kusudi wahesabiwe uadi-
lifu; **12** na baba ya uzao ulio-
tahiriwa, si kwa wale tu wanao-
shikamana na kutahiriwa, bali
pia kwa wale wanaotembea kwa
utaratibu katika hatua za imani
hiyo wakiwa katika hali ya ku-
totahiriwa ambayo baba[n] yetu
Abrahamu alikuwa nayo.

13 Kwa maana ahadi[o] ile
kwamba awe mrithi wa ulimwe-
ngu hakuipata Abrahamu au
uzao wake kupitia sheria, bali
ilikuwa kupitia uadilifu kwa
njia ya imani.[a] **14** Kwa maana
ikiwa wale ambao hushikamana
sana na sheria ni warithi, imani
imefanywa kuwa isiyofaa kitu
na ahadi imefutwa.[b] **15** Kwa
kweli Sheria hutokeza ghadha-
bu,[c] lakini mahali ambapo hapa-
na sheria, hapana pia kosa lo-
lote.[d]

16 Kwa hiyo ilitokana na
imani, ili iwe kulingana na fa-
dhili zisizostahiliwa,[e] kusudi
ahadi[f] iwe hakika kwa uzao[g]
wake wote, si kwa ule tu una-
oshikamana na Sheria, bali pia
kwa ule unaoshikamana na ima-
ni ya Abrahamu. (Yeye ndiye
baba[h] yetu sote, **17** kama ili-
vyoandikwa: "Nimekuweka
wewe kuwa baba ya mataifa me-
ngi.")[i] Hili lilikuwa machoni pa
Yule ambaye katika yeye aliku-
wa na imani, ndiyo, machoni
pa Mungu, anayewafanya wafu
kuwa hai[j] na kuyaita mambo
yasiyokuwako kana kwamba
yamekuwako.[k] **18** Ijapokuwa
alikuwa amepita hali ya kuwa
na tumaini,[l] bado kwa kutege-
mea tumaini alikuwa na imani,
ili awe baba ya mataifa[m] mengi
kwa kupatana na yale yaliyoku-
wa yamesemwa: "Ndivyo utaka-
vyokuwa uzao wako."[n] **19** Na,
ijapokuwa hakudhoofika kati-
ka imani, alifikiria juu ya mwi-
li wake mwenyewe, ukiwa sasa
tayari umekufa,[o] kwa kuwa ali-
kuwa mwenye umri wa kari-
bu miaka mia moja,[p] pia hali ya
kufa ya tumbo la uzazi la Sara.[q]
20 Lakini kwa sababu ya aha-
di[r] ya Mungu yeye hakusitasita
kwa ukosefu wa imani,[s] bali aka-
wa mwenye nguvu kwa imani[t]

SURA 4
a Mt 20:9
1Ti 5:18
b Ro 11:6
c Yoh 6:29
d Mdo 13:39
Ga 2:16
Ga 2:17
e Zb 85:2
Isa 43:25
f Zb 32:1
g Zb 32:2
2Ko 5:19
h Ro 3:30
i Ro 4:3
j 1Ko 7:19
k Mwa 17:1
Mwa 17:11
Mdo 7:8
l Lu 19:9
Ro 4:16
m Mwa 15:6
Ga 3:7
n Ga 3:29
o Mwa 12:3
Mwa 17:6
Mwa 18:18
Mwa 22:17

Safu ya 2
a Ebr 11:8
b Ga 3:18
c Ro 3:20
Ro 5:20
2Ko 3:7
Ga 3:19
d Ro 5:13
e Ro 3:24
f Ro 15:8
Ga 3:22
g Ro 9:8
Ga 3:29
h Ro 4:11
i Mwa 17:5
j Da 12:13
Lu 20:37
Efe 2:1
Ebr 11:19
k Lu 20:38
1Ko 1:28
1Pe 2:10
l Ebr 11:17
m Mwa 17:6
n Mwa 15:5
o Ebr 11:12
p Mwa 17:17
q Mwa 18:11
Ebr 11:11
r Ebr 6:13
s Ebr 3:19
t Ga 3:9
Ebr 11:34

yake, akimpa Mungu utukufu
21 na akiwa amesadikishwa ki-
kamili kwamba lile alilokuwa
ameahidi alikuwa na uwezo pia
wa kulifanya.[a] **22** Kwa saba-
bu hiyo "ikahesabiwa kwake
kuwa ni uadilifu."[b]
23 Hata hivyo, haikuandi-
kwa kwa ajili yake tu[c] kwamba
"ilihesabiwa[d] kwake," **24** bali
pia kwa ajili yetu ambao ita-
hesabiwa, kwa sababu tuna-
mwamini yeye aliyemfufua Yesu
Bwana wetu kutoka kwa wafu.[e]
25 Yeye alitolewa kwa ajili ya
makosa[f] yetu na kufufuliwa
kwa ajili ya kututangaza sisi
kuwa waadilifu.[g]

5 Basi, kwa kuwa sasa tume-
tangazwa kuwa waadilifu
kutokana na imani,[h] na tufu-
rahie amani[i] pamoja na Mungu
kupitia Bwana wetu Yesu Kri-
sto, **2** ambaye kupitia yeye
pia tumekaribia[j] kwa njia ya
imani kuingia katika fadhili hizi
zisizostahiliwa ambamo sasa tu-
nasimama; na acheni tufurahi,
kwa kutegemea tumaini[k] la utu-
kufu wa Mungu. **3** Na si hilo
tu, bali na tufurahi tukiwa kati-
ka dhiki,[l] kwa kuwa tunajua
kwamba dhiki hutokeza uvumi-
livu;[m] **4** nao uvumilivu, hali
yenye kukubaliwa;[n] nayo hali
yenye kukubaliwa, tumaini,[o]
5 nalo tumaini halikatishi ta-
maa;[p] kwa sababu upendo wa
Mungu[q] umemiminwa ndani ya
mioyo[r] yetu kupitia roho takati-
fu,[s] ambayo tulipewa.
6 Kwa maana, kwa kweli,
tulipokuwa tungali bado dhai-
fu,[t] Kristo alikufa wakati uli-
owekwa kwa ajili ya watu wa-
siomwogopa Mungu.[u] **7** Kwa
maana ni vigumu kwa yeyo-
te kufa kwa ajili ya mtu mwa-
dilifu;[a] kwa kweli, labda, mtu
anaweza kuthubutu kufa[b] kwa
ajili ya mtu mwema.[c] **8** Laki-
ni Mungu hupendekeza upendo[d]
wake mwenyewe kwetu kwa
kuwa, tulipokuwa tungali wate-
nda-dhambi, Kristo alikufa kwa
ajili yetu.[e] **9** Kwa hiyo, kwa
kuwa tumetangazwa kuwa wa-
adilifu sasa kwa damu yake,[f]
tutaokolewa kutokana na gha-
dhabu[g] kupitia yeye hata zaidi.
10 Kwa maana, ikiwa tulipo-
kuwa aduí[h] tulipatanishwa na
Mungu kupitia kifo cha Mwa-
na wake,[i] tutaokolewa kwa uhai
wake[j] hata zaidi, kwa kuwa
sasa tumepatanishwa. **11** Na
si hilo tu, bali pia tunafurahi
katika Mungu kupitia Bwana
wetu Yesu Kristo, ambaye ku-
pitia yeye sasa tumepokea huo
upatanisho.[k]
12 Hiyo ndiyo sababu, kama
vile kupitia mtu mmoja[l] dhambi
iliingia katika ulimwengu na
kifo[m] kupitia dhambi, na hivyo
kifo kikaenea kwa watu wote
kwa sababu wote walikuwa wa-
mefanya dhambi[n]—. **13** Kwa
maana kabla ya Sheria kuwako
dhambi ilikuwa katika ulimwe-
ngu, lakini mtu yeyote hahe-
sabiwi dhambi wakati hakuna
sheria.[o] **14** Hata hivyo, kifo
kilitawala kama mfalme tangu
Adamu mpaka Musa,[p] hata juu
ya wale ambao hawakuwa wa-
mefanya dhambi inayofanana
na kosa la Adamu,[q] aliye mfano
wake yeye aliyepaswa kuja.[r]
15 Lakini sivyo ilivyo kwa ile
zawadi kama ilivyokuwa kwa
lile kosa. Kwa maana ikiwa
kwa kosa la mtu mmoja we-
ngi walikufa, fadhili zisizostahi-
liwa za Mungu na zawadi yake

SURA 4
a Zb 115:3; Ebr 11:19
b Mwa 15:6; Yak 2:23
c Ro 15:4
d Flm 18
e Mdo 2:24; Mdo 13:30; 1Pe 1:21
f Isa 53:12; Mt 20:28
g Isa 53:11; 2Ko 5:21

SURA 5
h Mdo 13:39; Ro 3:26
i Isa 32:17; Ga 6:16; Efe 2:14
j Yoh 10:9; 2Ko 5:18; Efe 2:12; Efe 3:12; Ebr 10:19
k Ro 15:13; Ebr 3:6
l Mdo 5:41; Flp 2:17; 1Pe 3:14; 1Pe 4:13
m Mdo 5:42; Ebr 10:36
n 2Ti 2:15; Yak 1:12
o Flp 1:20
p Yos 21:45
q 1Yo 2:5; 2Yo 6
r 2Ko 1:22; Ga 4:6
s Efe 1:13; Tit 3:5
t Efe 2:5
u Mt 20:28

Safu ya 2
a Zb 49:8
b Yoh 15:13
c Mt 12:35
d Yoh 3:16; Efe 2:4; 1Yo 4:10
e Isa 53:12; 1Pe 3:18
f Mdo 13:39; Ga 2:16; Ebr 9:14
g 1Th 1:10; 1Th 5:9
h Isa 59:2; Kol 1:21
i 2Ko 5:18; Kol 1:22
j Mdo 15:11
k 2Ko 5:19; 1Yo 2:2
l Mwa 2:17; Mwa 3:6; Isa 43:27
m Mwa 3:19; 1Ko 15:21
n Zb 51:5; Eze 18:4; Ro 3:23
o Ro 4:15
p Ebr 2:15
q Ho 4:7; Ho 6:7
r 1Ko 15:45

ya bure ikiwa pamoja na fa-
dhili zisizostahiliwa kupitia
mtu mmoja[a] Yesu Kristo zilizi-
di sana kwa wengi.[b] **16** Pia, si-
vyo ilivyo kwa ile zawadi ya
bure[c] kama ilivyokuwa kwa
njia ambayo mambo yalitende-
ka kupitia mtu mmoja aliyefa-
nya dhambi.[d] Kwa maana hu-
kumu[e] ilitokana na kosa moja
katika hatia,[f] lakini zawadi ili-
tokana na makosa mengi katika
tangazo la uadilifu.[g] **17** Kwa
maana ikiwa kwa kosa la mtu
mmoja[h] kifo kilitawala kama
mfalme[i] kupitia mtu huyo, wale
wanaopokea wingi wa fadhi-
li zisizostahiliwa[j] na zawadi ya
bure[k] ya uadilifu watatawala
hata zaidi wakiwa wafalme[l] ka-
tika uzima kupitia mtu mmoja,
Yesu Kristo.[m]

18 Kwa hiyo, basi, kama vile
kupitia kosa moja matokeo kwa
watu wa namna zote yalikuwa
kuhukumiwa hatia,[n] vivyo hi-
vyo pia kupitia tendo moja la
kutetewa kuwa haki[o] matokeo
kwa watu wa namna zote[p] ni
wao kutangazwa kuwa waadili-
fu kwa ajili ya uzima.[q] **19** Kwa
maana kama vile kupitia kuto-
tii kwa mtu mmoja wengi[r] wa-
lifanywa watenda-dhambi, vi-
vyo hivyo pia kupitia kutii[s] kwa
mtu mmoja wengi[t] watafanywa
kuwa waadilifu.[u] **20** Basi She-
ria[v] iliingia kando ya hali hiyo
ili makosa yazidi.[w] Lakini ma-
hali ambapo dhambi ilizidi,[x] fa-
dhili zisizostahiliwa[y] zilizidi
hata zaidi. **21** Kwa kusudi
gani? Kwamba, kama vile dha-
mbi ilivyotawala kama mfa-
lme pamoja na kifo,[z] vivyo hi-
vyo pia fadhili zisizostahiliwa[a]
zitawale kama mfalme kupitia
uadilifu kwa tazamio la uzima

SURA 5

a Isa 53:11
Ebr 2:9
b Mt 20:28
Tit 3:4
c Ro 6:23
d Mwa 2:17
Mwa 3:6
e Mwa 3:17
f Mwa 3:19
1Ko 11:32
g Ro 4:25
h Ro 5:12
i Ro 5:14
j 2Ko 9:8
k Ro 3:24
2Ko 9:15
Yak 1:17
l Ufu 5:10
Ufu 20:4
m 1Pe 3:18
Ufu 1:5
n 1Ko 15:21
o Ro 4:25
p Ro 1:16
Ga 3:28
1Ti 2:4
q Yoh 10:10
Ro 3:25
r Zb 51:5
Ro 5:12
s Ebr 5:8
t Ebr 2:10
u Isa 53:11
v Ro 3:20
w Ga 3:19
x Yoh 15:22
y 1Ti 1:14
z 1Ko 15:56
a Yoh 1:17

Safu ya 2

a Yoh 3:16
1Yo 4:9

SURA 6

b Ro 3:8
c Kol 2:20
1Pe 2:24
d Ebr 10:26
e 1Ko 12:13
Ga 3:27
f Mk 10:38
1Ko 15:29
g Mk 10:39
2Ko 4:10
Kol 2:12
h 1Ko 6:14
2Ti 2:11
i 2Ko 5:17
Ga 6:15
Efe 3:16
Kol 3:10
1Yo 3:14
j Flp 3:10
Ufu 2:10
k 1Ko 15:42
1Ko 15:49
Efe 2:6
l Ga 5:24
Kol 3:5
m Kol 2:11
Kol 3:5
n 2Ko 7:1
Ga 5:1
o Isa 40:2
Lu 23:41
Mdo 13:39
p 2Ti 2:11
q Ufu 1:18

wa milele[a] kupitia Yesu Kristo
Bwana wetu.

6 Kwa hiyo, tuseme nini? Je,
tuendelee kuwa katika dha-
mbi, ili fadhili zisizostahiliwa
ziwe nyingi?[b] **2** Hilo lisitende-
ke kamwe! Kwa kuwa tulikufa
kuhusiana na dhambi,[c] tu-
taendeleaje kuishi tena katika
hiyo?[d] **3** Au je, hamjui kwa-
mba sisi sote tuliobatizwa kati-
ka Kristo Yesu[e] tulibatizwa ka-
tika kifo chake?[f] **4** Kwa hiyo
tulizikwa[g] pamoja naye kupi-
tia ubatizo wetu katika kifo
chake, ili, kama vile Kristo ali-
vyofufuliwa kutoka kwa wafu
kupitia utukufu wa Baba,[h] vi-
vyo hivyo sisi pia tunapaswa tu-
tembee katika hali mpya ya uzi-
ma.[i] **5** Kwa maana ikiwa tu-
meungana pamoja naye katika
mfano wa kifo chake,[j] hakika
sisi pia tutaunganishwa pamo-
ja naye katika mfano wa ufu-
fuo[k] wake; **6** kwa sababu tu-
najua kwamba utu wetu wa za-
mani ulitundikwa mtini pamoja
naye,[l] ili mwili wetu wenye dha-
mbi ufanywe kuwa usiotenda,[m]
ili tusiendelee tena kuwa watu-
mwa wa dhambi.[n] **7** Kwa maa-
na yeye ambaye amekufa ameo-
ndolewa hatia ya dhambi yake.[o]
8 Zaidi ya hayo, ikiwa tu-
mekufa pamoja na Kristo, tu-
naamini kwamba tutaishi pia
pamoja naye.[p] **9** Kwa maana
tunajua kwamba Kristo hafi
tena,[q] kwa kuwa sasa ame-
kwisha kufufuliwa kutoka kwa
wafu;[r] kifo si bwana juu yake
tena. **10** Kwa maana kifo ali-
chokufa, alikufa kuhusiana na
dhambi mara moja kwa waka-
ti wote;[s] lakini uzima anaoi-
shi, anaishi kwa kuhusiana na

r Mdo 13:34; 1Ko 15:20; s Ebr 9:28; 1Pe 3:18.

Mungu.[a] **11** Vivyo hivyo ninyi pia: jihesabuni wenyewe
kuwa wafu[b] kwelikweli kuhusiana na dhambi lakini walio hai[c]
kuhusiana na Mungu kwa njia
ya Kristo Yesu.

12 Kwa hiyo msiache dhambi iendelee kutawala kama
mfalme[d] katika miili yenu inayoweza kufa hivi kwamba mzitii tamaa[e] zake. **13** Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu
kwa dhambi[f] kuwa silaha za ukosefu wa uadilifu,[g] bali jitoeni
wenyewe kwa Mungu kama walio hai[h] kutoka kwa wafu, pia viungo vyenu kwa Mungu kuwa
silaha[i] za uadilifu. **14** Kwa maana dhambi haipaswi kuwa
bwana juu yenu, kwa kuwa ninyi hamko chini ya sheria[j] bali
chini ya fadhili zisizostahiliwa.[k]

15 Tuseme nini basi? Je, tufanye dhambi kwa sababu hatuko chini ya sheria[l] bali chini
ya fadhili zisizostahiliwa?[m] Hilo lisitendeke kamwe! **16** Je, hamjui kwamba ikiwa mnaendelea kujitoa wenyewe kwa yeyote kuwa watumwa ili kumtii
yeye, ninyi ni watumwa wake kwa sababu mnamtii yeye,[n] ama
watumwa wa dhambi[o] kwa kutazamia kifo[p] ama wa utii[q] kwa
kutazamia uadilifu?[r] **17** Lakini ni shukrani kwa Mungu kwamba mlikuwa watumwa wa dhambi lakini kutoka moyoni mkawa wenye kutii namna ile ya fundisho ambayo mliwekwa chini
yake.[s] **18** Ndiyo, kwa kuwa mliwekwa huru[t] kutoka katika dhambi, mlikuja kuwa watumwa[u] wa uadilifu.[v] **19** Ninasema kwa maneno ya kibinadamu
kwa sababu ya udhaifu wa mwili[w] wenu: kwa maana kama mlivyovitoa viungo[x] vyenu kuwa
watumwa wa ukosefu wa usafi[a] na uasi-sheria kwa kutazamia uasi-sheria, basi sasa vitoeni viungo vyenu viwe watumwa
wa uadilifu kwa kutazamia utakatifu.[b] **20** Kwa maana mlipokuwa watumwa wa dhambi,[c]
mlikuwa huru kwa habari ya uadilifu.

21 Basi, ni tunda[d] gani ambalo kwa kawaida mlikuwa nalo
wakati huo? Mambo[e] ambayo sasa mnayaonea aibu. Kwa maana mwisho wa mambo hayo
ni kifo.[f] **22** Hata hivyo, sasa, kwa sababu mliwekwa huru kutoka katika dhambi lakini mkawa watumwa kwa Mungu,[g] mnapata tunda[h] lenu katika utakatifu, na mwisho ni uzima wa milele.[i] **23** Kwa maana mshahara
ambao dhambi hulipa ni kifo,[j] lakini zawadi[k] ambayo Mungu
hutoa ni uzima wa milele[l] kupitia Kristo Yesu Bwana wetu.[m]

7 Akina ndugu, je, inawezekana kwamba hamjui (kwa
maana ninasema na wale wanaoijua sheria,) kuwa Sheria ni
bwana juu ya mtu wakati tu anapokuwa hai?[n] **2** Kwa mfano, mwanamke aliyeolewa amefungwa na sheria kwa mume
wake akiwa hai; lakini mume wake akifa, yeye amefunguliwa
kutoka katika sheria ya mume wake.[o] **3** Hivyo, basi, mume
wake anapokuwa hai, mwanamke huyo ataitwa mzinzi ikiwa
atakuwa wa mwanamume mwingine.[p] Lakini mume wake akifa, yeye yuko huru kutoka katika sheria ya mume, hivi kwamba mwanamke huyo si mzinzi
akiwa wa mwanamume mwingine.[q]

4 Hivyo, ndugu zangu, ninyi pia mlifanywa wafu kuhusia-

SURA 6
a 1Pe 4:2
b Kol 3:3
c 1Pe 2:24
d Mwa 4:7
Zb 119:133
e Yak 4:1
f Ro 7:5
g 1Ko 6:15
h Ro 12:1
i 2Ko 10:4
Efe 6:17
j Ro 7:6
Ga 5:18
Kol 2:14
k Yoh 1:17
l 1Ko 9:21
m Ro 5:21
n 2Pe 2:19
o Yoh 8:34
p Eze 18:4
Ro 6:23
q Ebr 5:9
r Ro 1:17
s 2Ti 1:13
t Yoh 8:32
Ga 5:1
u 1Ko 7:22
v 1Pe 2:24
w Ro 7:23
x Mt 18:8

Safu ya 2
a 1Ko 6:15
b Ro 12:1
c Yoh 8:34
d Yer 12:13
e Ga 5:19
f Ro 8:6
g Ro 8:15
h Ga 5:22
i 1Ko 9:25
j Mwa 2:17
Eze 18:4
k Ro 3:24
l Mt 25:46
1Pe 1:4
m 1Ti 1:16
1Yo 2:2
Yud 21

SURA 7
n Ro 3:19
o Hes 30:8
1Ko 7:39
p Mt 5:32
Mt 19:9
Mk 10:12
Lu 16:18
q 1Ko 7:9
1Ti 5:14

na na Sheria[a] kupitia mwili wa
Kristo, ili muwe wa mwingi-
ne,[b] muwe wa yule aliyefufuli-
wa kutoka kwa wafu,[c] ili tumza-
lie Mungu matunda.[d] **5** Kwa
maana tulipokuwa tunapa-
tana na mwili,[e] tamaa zenye
dhambi zilizotokezwa kupitia
Sheria zilikuwa zikifanya kazi
katika viungo vyetu ili tuza-
lie kifo matunda.[f] **6** Lakini
sasa tumefunguliwa kutoka ka-
tika Sheria,[g] kwa sababu tume-
kufa[h] kwa kile ambacho kiliku-
wa kimetufunga, ili tuwe watu-
mwa[i] katika maana mpya kwa
roho,[j] wala si katika maana ya
zamani kwa njia ya sheria zilizo-
andikwa.[k]

7 Basi, tuseme nini? Je, She-
ria ni dhambi?[l] Isiwe hivyo ka-
mwe! Kwa kweli singejua dha-
mbi[m] kama isingekuwa kwa sa-
babu ya Sheria; na, kwa mfano,
mimi singejua tamaa[n] kama
Sheria haingesema: "Usitama-
ni."[o] **8** Lakini dhambi, kwa
kuchochewa na amri hiyo,[p] ili-
fanyiza ndani yangu tamaa ya
kila namna, kwa maana bila
sheria dhambi ilikuwa imeku-
fa.[q] **9** Kwa kweli, wakati
mmoja nilikuwa hai bila she-
ria;[r] lakini amri ilipofika,[s] dha-
mbi ikawa hai tena, lakini mimi
nikafa.[t] **10** Na amri iliyokuwa
ya kuongoza kwenye uzima,[u] ni-
liiona hii kuwa ya kuongoza
kwenye kifo.[v] **11** Kwa maa-
na dhambi, kwa kuchochewa
na amri, ilinishawishi[w] na kuni-
ua kupitia hiyo. **12** Kwa saba-
bu hiyo, kwa upande wake, She-
ria ni takatifu,[x] na amri ni taka-
tifu na ya uadilifu[y] na njema.[z]

13 Basi, je, lililo jema lilikuja
kuwa kifo kwangu? Isiwe hi-
vyo kamwe! Lakini dhambi ili-
kuwa hivyo, ili ionyeshwe kuwa
dhambi ndiyo inayoniletea kifo
kupitia lile lililo jema;[a] ili dha-
mbi iwe dhambi zaidi kupitia
amri.[b] **14** Kwa maana tuna-
jua kwamba Sheria ni ya kiro-
ho;[c] lakini mimi ni wa kimwi-
li, nimeuzwa chini ya dhambi.[d]
15 Kwa maana lile ninalofa-
nya silijui. Kwa maana lile ni-
nalolitaka, hilo sizoei kulifanya;
bali lile ninalochukia ndilo ni-
nalofanya. **16** Hata hivyo, iki-
wa lile ambalo sitaki ndilo nina-
lofanya,[e] nakubali kwamba She-
ria ni nzuri.[f] **17** Lakini sasa
anayefanya hilo si mimi tena,
bali ni dhambi inayokaa nda-
ni yangu.[g] **18** Kwa maana na-
jua kwamba ndani yangu, yaa-
ni, ndani ya mwili wangu, hali-
kai jambo lolote jema;[h] kwa ma-
ana nina uwezo wa kutaka,[i] bali
uwezo wa kufanya[j] yaliyo mazu-
ri haupo. **19** Kwa maana lile
jema ninalotaka silifanyi,[k] bali
lile baya nisilotaka ndilo nina-
lozoea kulifanya. **20** Basi, iki-
wa lile nisilotaka ndilo ninalo-
fanya, anayelifanya hilo si mimi
tena, bali ni ile dhambi inayokaa
ndani yangu.[l]

21 Basi, mimi naona sheria
hii katika hali yangu: kwa-
mba ninapotaka kufanya ya-
liyo sawa,[m] yaliyo mabaya yapo
pamoja nami.[n] **22** Kwa kweli
naipenda[o] sheria ya Mungu ku-
lingana na mtu[p] niliye kwa nda-
ni, **23** lakini mimi naona nda-
ni ya viungo[q] vyangu sheria nyi-
ngine ikipigana[r] na sheria ya
akili[s] yangu na kunichukua ma-
teka kwa sheria ya dhambi[t] ili-
yo ndani ya viungo vyangu.
24 Maskini mimi! Ni nani ata-
kayeniokoa kutoka katika
mwili unaopatwa na kifo hiki?[u]

SURA 7

a Ro 6:14
Ga 2:19
Kol 2:14
b Zb 45:10
2Ko 11:2
c Mdo 5:30
2Ko 5:15
d Ga 5:22
Kol 1:10
e Ga 5:19
f Ro 6:21
Yak 1:15
g Ro 10:4
Efe 2:15
Kol 2:14
h Ga 2:19
i Ro 12:11
j 2Ko 3:6
k Ga 3:10
Kol 2:14
l Ro 7:14
m Ro 3:20
Ga 3:19
n Mik 2:2
Mdo 20:33
o Kut 20:17
Kum 5:21
Efe 5:3
p Ro 4:15
Ro 5:20
q 1Ko 15:56
r Ro 11:1
Ebr 7:10
s Ebr 7:11
t 2Ko 3:6
u Law 18:5
Eze 20:11
Lu 10:28
v 2Ko 3:7
w Ebr 3:13
x Zb 19:8
Ga 3:21
y Met 2:9
Ro 10:5
z Kum 4:8

Safu ya 2

a 1Ko 15:56
b Ro 5:13
c 1Ko 10:4
d Zb 51:5
Yoh 8:34
Ro 6:16
e Zb 51:3
Lu 18:13
f 1Ti 1:8
g Mwa 8:21
h Mwa 6:5
Isa 64:6
i Mt 26:41
j Ayu 14:4
k Yak 4:17
l Mhu 7:20
m Zb 34:14
1Pe 3:11
n Mhu 7:29
Yer 17:9
Lu 5:22
o Zb 1:2
p 2Ko 4:16
Efe 3:16
Efe 4:23
q Ro 6:13
r Yak 4:1
s Ga 5:17
t Yoh 8:34
u Ro 6:6
Ro 8:10

25 Shukrani kwa Mungu kupitia Yesu Kristo Bwana wetu![a]
Basi, kwa akili yangu mimi
mwenyewe ni mtumwa wa sheria[b] ya Mungu, lakini kwa mwili
wangu mimi ni mtumwa wa sheria ya dhambi.[c]

8 Kwa hiyo wale walio katika muungano na Kristo
Yesu hawana hukumu ya hatia.[d] **2** Kwa maana sheria[e] ya
ile roho[f] ambayo hutokeza uzima[g] katika muungano na Kristo
Yesu imewaweka ninyi huru[h]
kutoka katika sheria ya dhambi
na kifo.[i] **3** Kwa maana, Sheria[j] ikiwa haina uwezo, huku
ilipokuwa dhaifu[k] kupitia mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwana[l] wake mwenyewe akiwa katika mfano wa mwili[m] wenye
dhambi[n] na kuhusu dhambi, alihukumu dhambi katika mwili, **4** ili takwa la uadilifu la
Sheria litimizwe[o] ndani yetu sisi
tunaotembea, si kupatana na
mwili, bali kupatana na roho.[p]
5 Kwa maana wale wanaopatana
na mwili hukaza akili zao juu
ya mambo ya mwili,[q] lakini wale
wanaopatana na roho juu ya
mambo ya roho.[r] **6** Kwa maana kukaza akili juu ya mwili humaanisha kifo,[s] bali kukaza akili juu ya roho[t] humaanisha
uzima na amani; **7** kwa sababu kukaza akili juu ya mwili
humaanisha uadui[u] na Mungu,
kwa maana mwili haujitiishi[v]
chini ya sheria ya Mungu, nao
kwa kweli hauwezi kujitiisha.
8 Kwa hiyo wale wanaopatana
na mwili[w] hawawezi kumpendeza Mungu.

9 Hata hivyo, ninyi hampatani na mwili, bali mnapatana na roho,[x] ikiwa kweli roho
ya Mungu inakaa ndani yenu.[y]
Lakini ikiwa mtu yeyote hana
roho[a] ya Kristo, mtu huyo si
wake. **10** Lakini ikiwa Kristo
yuko katika muungano pamoja
na ninyi,[b] mwili kwa kweli umekufa kwa sababu ya dhambi,
bali roho ni uzima[c] kwa sababu ya uadilifu. **11** Basi, ikiwa
roho ya yule aliyemfufua Yesu
kutoka kwa wafu inakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu kutoka kwa wafu[d] ataifanya pia miili yenu inayoweza
kufa iwe hai[e] kupitia roho yake
inayokaa ndani yenu.

12 Basi, akina ndugu, sisi
tuna wajibu, si kwa mwili
ili tuishi kupatana na mwili;[f]
13 kwa maana ikiwa mnaishi
kupatana na mwili hakika ninyi mtakufa;[g] bali mkiyaua mazoea ya mwili[h] kwa roho, mtaishi. **14** Kwa maana wote wanaoongozwa na roho ya Mungu, hao ndio wana wa Mungu.[i]
15 Kwa maana hamkupokea
roho ya utumwa inayosababisha woga[j] tena, bali mlipokea
roho[k] ya kufanywa kuwa wana,[l]
roho ambayo kupitia hiyo tunapaaza sauti: *"Abba,*[m] Baba!"
16 Roho[n] yenyewe hutoa ushahidi[o] pamoja na roho[p] yetu kwamba sisi ni watoto wa Mungu.[q]
17 Basi, ikiwa sisi ni watoto, sisi
pia ni warithi: warithi wa Mungu kwelikweli, lakini warithi[r]
pamoja na Kristo, mradi tu tunateseka[s] pamoja ili pia tutukuzwe pamoja.[t]

18 Kwa sababu hiyo nahesabu kwamba mateso[u] ya majira haya si kitu kwa kulinganisha na utukufu[v] utakaofunuliwa ndani yetu. **19** Kwa

SURA 7

a Ro 6:17
1Ko 15:57
b Zb 19:7
Ga 5:18
c Ga 5:17

SURA 8

d Kol 1:22
1Yo 3:24
e Yak 1:25
f Ga 5:16
g Yoh 5:24
h Yoh 8:32
Ebr 10:14
i Ro 7:9
2Ko 3:6
j Ro 3:20
Ebr 7:11
k Ebr 7:18
l 1Yo 4:9
m Yoh 1:14
Ga 4:4
Ebr 4:15
n 2Ko 5:21
o Ro 3:31
p Ga 5:16
Ga 5:18
q Yoh 3:6
Ga 5:19
r 1Ko 2:15
Ga 5:22
s Ro 6:21
Ebr 9:14
t Ga 6:8
u Zb 5:4
Isa 59:2
Kol 1:21
Yak 4:4
v Ro 7:14
w 1Ko 3:3
x Ga 5:25
y 1Ko 3:16

Safu ya 2

a Ga 4:6
b Yoh 15:4
1Yo 2:6
1Yo 3:6
c Ga 2:20
1Pe 4:6
d Mdo 2:24
1Ko 6:14
e Efe 2:5
f Ga 5:19
g Ro 8:6
h 1Ko 9:27
Ga 5:24
Ga 6:8
Efe 4:22
Kol 3:5
i Yoh 1:12
Yoh 3:5
Yoh 3:8
Ebr 2:11
j Ebr 2:15
k 1Ko 2:12
2Ko 1:22
2Ti 1:7
l Ga 4:5
m Ga 4:6
n Yoh 14:17
1Ko 2:10
Tit 3:6
o 1Yo 5:7
p Mdo 17:16
Ro 1:9
1Ko 2:11

q Yoh 1:12; Ga 3:26; 1Yo 3:2; r Lu 12:32; Mdo 26:18; Ga 3:29; Ufu 21:7; s Flp 1:29; Kol 1:24; t 1Ko 15:53; 2Ti 2:11; Ufu 3:21; u 1Pe 4:13; v 2Ko 4:17; Flp 3:8.

maana uumbaji[a] unangojea na
kutazamia kwa hamu[b] kufu-
nuliwa kwa wana wa Mungu.[c]
20 Kwa maana uumbaji ulitii-
shwa chini ya ubatili,[d] si kwa
mapenzi yake wenyewe bali ku-
pitia yeye aliyeutiisha hivyo,
juu ya msingi wa tumaini[e]
21 kwamba uumbaji[f] wenye-
we pia utawekwa huru[g] kuto-
ka katika utumwa wa uhari-
bifu na kuwa na uhuru wenye
utukufu wa watoto wa Mungu.
22 Kwa maana tunajua kwa-
mba uumbaji wote unaendelea
kuugua pamoja na kuwa katika
maumivu pamoja mpaka sasa.
23 Si hilo tu, bali sisi wenyewe
pia tulio na matunda ya kwa-
nza,[h] yaani, ile roho, ndiyo, sisi
wenyewe tunaugua[i] ndani yetu
wenyewe, huku tukingojea kwa
bidii kufanywa kuwa wana,[j]
kuachiliwa huru kutoka kati-
ka miili yetu kwa njia ya fidia.
24 Kwa maana tuliokolewa ka-
tika tumaini hili;[k] lakini tu-
maini linaloonekana si tumaini,
kwa maana mtu anapoona kitu,
je, yeye hukitumainia? **25** La-
kini tukitumainia[l] kile amba-
cho hatuoni,[m] sisi huendelea ku-
kingojea kwa uvumilivu.[n]
26 Vivyo hivyo roho[o] pia
hujiunga kutoa msaada kwa
ajili ya udhaifu wetu;[p] kwa
maana lile tatizo kuhusu tu-
nalohitaji kusali hatujui,[q] la-
kini roho[r] yenyewe hutuo-
mbea pamoja na kuugua ku-
sikotamkwa. **27** Lakini yeye
ambaye huichunguza mioyo[s]
anajua ni nini maana ya roho,[t]
kwa sababu inaomba kupata-
na na Mungu kwa ajili ya wata-
katifu.[u]
28 Basi tunajua kwamba Mu-
ngu hufanya kazi[v] zake zote

SURA 8

a Kol 1:23
Ebr 11:13
b Met 13:12
c 1Yo 3:2
d Mwa 3:19
Zb 51:5
Mhu 1:2
e Mwa 3:15
Mdo 24:15
f 1Ti 2:4
g Yoh 8:32
1Ko 15:22
2Pe 3:13
h Flp 3:11
Ufu 20:6
i 2Ko 5:2
j Ga 4:5
Efe 1:5
1Pe 1:4
Ufu 21:7
k Efe 1:13
l 1Pe 1:3
m 2Ko 5:7
n Ro 5:4
o Yoh 15:26
1Ko 2:12
p Yoh 14:16
Yoh 16:7
q Lu 11:1
r 2Sa 23:2
s Yer 11:20
Mdo 1:24
t Yoh 6:63
Yoh 14:17
1Ko 2:10
1Ko 2:14
2Ti 3:16
u 1Pe 1:15
v Zb 145:17
Yoh 9:3

Safu ya 2

a Ro 9:11
Efe 1:11
2Ti 1:9
b 1Ko 15:23
c Mwa 3:15
d Yoh 13:15
e Yoh 17:23
Ro 6:5
1Ko 15:49
Efe 4:24
f Zb 89:27
Ebr 1:6
g Mt 25:40
Ebr 2:11
1Yo 3:2
h Efe 1:5
i Flp 3:14
1Th 2:12
Ebr 3:1
j Ro 5:18
1Ko 6:11
Tit 3:7
k 2Ko 3:7
2Ko 3:18
2Ko 4:6
l Zb 118:6
1Yo 4:4
m Yoh 3:16
n Ro 3:25
2Ko 5:21
1Yo 4:9
o Efe 2:4
p Isa 50:8
Kol 1:22
q Mdo 13:39
Ebr 10:17
r Zb 110:1
s Ebr 7:25
1Yo 2:1
t Yoh 15:10
u 2Ko 4:9
v Zb 44:22

zishirikiane pamoja kwa aji-
li ya mema ya wale wanaompe-
nda Mungu, wale ambao wame-
itwa kulingana na kusudi lake;[a]
29 kwa sababu wale aliowapa
utambuzi[b] wake wa kwanza pia
aliwaagiza kimbele[c] wafananis-
hwe[d] na mfano[e] wa Mwana
wake, ili awe mzaliwa wa kwa-
nza[f] kati ya ndugu[g] wengi.
30 Zaidi ya hayo, wale aliowaa-
giza kimbele[h] hao ndio aliowa-
ita[i] pia; na wale aliowaita hao
ndio aliowatangaza kuwa waa-
dilifu[j] pia. Mwishowe wale alio-
watangaza kuwa waadilifu hao
ndio aliowatukuza pia.[k]
31 Basi, tuseme nini kuhu-
su mambo haya? Ikiwa Mu-
ngu yuko upande wetu, ni
nani atakayekuwa dhidi yetu?[l]
32 Yeye ambaye hakujizuia
hata Mwana[m] wake mwenyewe
bali alimtoa kwa ajili yetu sisi
sote,[n] kwa nini yeye pia pamo-
ja naye hatatupa sisi kwa fadhi-
li vitu vingine vyote?[o] **33** Ni
nani atakayefanya shtaka juu
ya waliochaguliwa wa Mungu?[p]
Mungu Ndiye anayewatangaza
kuwa waadilifu.[q] **34** Ni nani
ambaye atahukumu kuwa na
hatia? Kristo Yesu ndiye aliye-
kufa, ndiyo, afadhali zaidi ku-
sema yeye ndiye aliyefufuliwa
kutoka kwa wafu, aliye kwenye
mkono wa kuume[r] wa Mungu,
ambaye pia hutuombea.[s]
35 Ni nani atakayetutenga na
upendo wa Kristo?[t] Je, ni dhi-
ki au taabu au mateso au njaa
au uchi au hatari au upanga?[u]
36 Kama ilivyoandikwa: "Kwa
ajili yako tunauawa mchana ku-
twa, tumehesabiwa kuwa ko-
ndoo wa kuchinjwa."[v] **37** Ki-
nyume chake, katika mambo
haya yote tunatokea tukiwa

tumeshinda[a] kabisa kupitia yeye
aliyetupenda. **38** Kwa maana
nimesadiki kwamba wala kifo
wala uzima[b] wala malaika[c] wala
serikali[d] wala mambo yaliyo-
po sasa wala mambo yataka-
yokuja wala nguvu[e] **39** wala
kimo wala kina wala uumba-
ji mwingine wowote havitawe-
za kututenga na upendo wa Mu-
ngu ulio katika Kristo Yesu Bwa-
na wetu.[f]

9 Ninasema kweli[g] katika
Kristo; sisemi uwongo,[h]
kwa kuwa dhamiri yangu inani-
tolea ushahidi katika roho taka-
tifu, **2** kwamba nina huzuni
kubwa na maumivu yasiyokoma
moyoni mwangu.[i] **3** Kwa ma-
ana ningetaka mimi mwenyewe
nitenganishwe na Kristo, niwe
aliyelaaniwa kwa ajili ya ndu-
gu zangu,[j] jamaa zangu kuli-
ngana na mwili,[k] **4** ambao ni
Waisraeli,[l] ambao kule kufa-
nywa wana[m] ni kwao na utu-
kufu[n] na maagano[o] na kupewa
Sheria[p] na utumishi mtakati-
fu[q] na ahadi;[r] **5** ambao maba-
bu[s] ni wao na ambao Kristo ali-
toka kwao kulingana na mwi-
li:[t] Mungu,[u] aliye juu ya wote,
abarikiwe milele. Amina.

6 Hata hivyo, si kwamba neno
la Mungu lilikuwa limeshindwa.[v]
Kwa maana si wote wanaotoka-
na na Israeli ni "Israeli" kikwe-
li.[w] **7** Wala si wote walio wato-
to kwa sababu wao ni uzao wa
Abrahamu,[x] bali: "Ule utakaoi-
twa 'uzao wako' utakuwa kupi-
tia Isaka."[y] **8** Yaani, watoto
kwa njia ya mwili[z] si watoto
wa Mungu kikweli,[a] bali wato-
to kwa njia ya ahadi[b] huhesa-
biwa kuwa ndio uzao. **9** Kwa
maana neno la ahadi lilikuwa

SURA 8

a Yoh 16:33
b 1Ko 3:22
c 1Pe 3:22
d Efe 1:21
e Efe 6:12
f 2Th 3:5

SURA 9

g 1Ti 2:7
h Ga 1:20
i Ro 10:1
j Kut 32:32
k Ro 16:7
Ro 16:21
l 2Ko 11:22
Flp 3:5
m Kut 4:22
n Kum 26:19
o Mdo 3:25
Mdo 7:8
p Kut 24:12
q Mdo 26:7
Ebr 9:1
r Mdo 13:32
Ro 4:13
s Kum 10:15
t Mt 1:17
u Zb 103:19
v Hes 23:19
w Mt 23:38
Ro 2:28
Ufu 2:9
x Yoh 8:39
Ga 3:29
y Mwa 21:12
Ebr 11:18
z Isa 57:4
Ga 4:23
a Yoh 1:13
b Isa 54:1
Ga 4:28

Safu ya 2

a Mwa 18:14
b Mwa 25:24
c Zb 139:16
d Ro 8:28
Ebr 5:4
e Mwa 25:23
f Mal 1:3
Ebr 12:16
g Kum 32:4
2Nya 19:6
Ayu 34:10
h Kut 33:19
i Zb 115:3
j Kum 4:31
Tit 3:5
k Kut 9:16
l Kut 20:6
m Kut 10:1
Kut 14:4
n 2Nya 20:6
Ayu 23:13
Da 4:35
o Ro 2:1
p Ayu 40:2

hivi: "Wakati huu nitakuja na
Sara atapata mwana."[a] **10** La-
kini si tukio hilo peke yake,
bali pia Rebeka alipochukua
mimba ya mapacha[b] kwa yule
mwanamume mmoja, Isaka
babu yetu: **11** kwa maana
walipokuwa bado hawajazali-
wa wala kufanya jambo lolote
jema au baya,[c] ili kusudi la Mu-
ngu kuhusu kuchagua liende-
lee kutegemea, si matendo, bali
Yeye ambaye huita,[d] **12** Re-
beka aliambiwa: "Mkubwa ata-
kuwa mtumwa wa mdogo."[e]
13 Kama ilivyoandikwa: "Ni-
limpenda Yakobo, lakini nili-
mchukia Esau."[f]

14 Basi, tuseme nini? Je, Mu-
ngu ana ukosefu wa haki?[g] Isi-
we hivyo kamwe! **15** Kwa ma-
ana yeye anamwambia Musa:
"Nitamwonyesha rehema yeyo-
te ninayetaka kumwonyesha
rehema, nami nitamwonyesha
huruma yeyote ninayetaka ku-
mwonyesha huruma."[h] **16** Hi-
vyo basi, haitegemei yule
anayetaka wala yule anayeki-
mbia, bali hutegemea Mungu,[i]
aliye na rehema.[j] **17** Kwa ma-
ana Andiko linamwambia Fa-
rao: "Kwa sababu hii nimekua-
cha ubaki, ili kuhusiana na wewe
nionyeshe nguvu zangu, na ili
jina langu litangazwe katika
dunia yote."[k] **18** Hivyo basi,
yeye humwonyesha rehema yule
ambaye yeye anataka,[l] lakini
yeye ambaye anataka kumwa-
cha humwacha awe mkaidi.[m]

19 Kwa hiyo utaniambia:
"Kwa nini bado analaumu? Kwa
maana ni nani ambaye amepi-
nga mapenzi yake yaliyo wazi?"[n]
20 Basi, Ee mwanadamu,[o] kwa
kweli wewe ni nani ndipo
uthubutu kumjibu Mungu?[p] Je,

kitu kilichofinyangwa kitamwambia yeye aliyekifinyanga, "Kwa nini ulinifanya mimi hivi?"[a] **21** Kwani? Je, mfinyanzi[b] hana mamlaka juu ya udongo wa mfinyanzi kufanya kutokana na donge lilelile chombo kimoja kwa matumizi yenye kuheshimika, kingine kwa matumizi yasiyo na heshima?[c] **22** Basi, ikiwa Mungu, ingawa alikuwa na nia ya kuonyesha ghadhabu yake na kujulisha nguvu zake, alivumilia kwa ustahimilivu mwingi vyombo vya ghadhabu vilivyofanywa kuwa vyenye kufaa kwa ajili ya uharibifu,[d] **23** ili ajulishe utajiri[e] wa utukufu wake juu ya vyombo[f] vya rehema, alivyotayarisha kimbele kwa ajili ya utukufu,[g] **24** yaani, sisi, ambao alituita si kutoka kati ya Wayahudi peke yao bali pia kutoka kati ya mataifa,[h] kuna ubaya gani? **25** Ni kama anavyosema pia katika Hosea: "Wale ambao si watu wangu[i] nitawaita 'watu wangu,' na mwanamke ambaye hakuwa mpendwa nitamwita 'mpendwa';[j] **26** na mahali ambapo waliambiwa, 'Ninyi si watu wangu,' hapo wataitwa 'wana wa Mungu aliye hai.'"[k]

27 Zaidi ya hayo, Isaya anapaaza sauti kuhusu Israeli: "Ijapokuwa hesabu ya wana wa Israeli huenda ikawa kama mchanga wa bahari,[l] ni mabaki watakaookolewa.[m] **28** Kwa maana Yehova atatoza hesabu duniani, na kuimaliza na kuifupisha."[n] **29** Pia, kama Isaya alivyokuwa amesema wakati uliotangulia: "Kama Yehova wa majeshi[o] hangalituachia sisi uzao, tungalikuwa kama Sodoma, nasi tungalifanywa kama Gomora."[p]

SURA 9

a Isa 29:16; Isa 45:9
b Isa 64:8; Yer 18:6
c 2Ti 2:20
d 1Th 5:9
e Kol 1:27
f Mdo 9:15
g Flp 4:19
h Ro 11:13; Efe 3:6
i Efe 2:12
j Ho 2:23; Mt 21:43; 1Pe 2:10
k Ho 1:10; Ga 3:26
l Mwa 22:17; 1Fa 4:20
m Isa 10:22; Ro 11:5
n Isa 10:23
o Zb 103:21
p Isa 1:9; Yer 50:40

Safu ya 2

a Ro 10:20
b Ro 1:17; Ro 4:11; Flp 3:9
c Ga 2:21; Ga 5:4
d Ga 2:16
e Lu 20:18; 1Ko 1:23
f Zb 118:22; Mt 21:42; 1Pe 2:6
g Isa 8:14
h Isa 28:16; Isa 49:23

SURA 10

i Ro 9:3
j Mt 7:22; Mdo 21:20; Ga 1:14; Flp 3:6
k Efe 1:17
l Ro 1:17
m Lu 16:15; Lu 18:9; Flp 3:9
n Mt 15:6; Lu 7:30
o Mt 5:17; Ro 7:6; Efe 2:15; Kol 2:14
p Mdo 13:39; Ga 3:24
q Law 18:5; Ne 9:29; Eze 20:11; Ga 3:12
r Kum 9:4
s Kum 30:12
t Ebr 8:1
u Kum 30:13; Ufu 20:1
v Mt 27:64

30 Basi, tuseme nini? Kwamba watu wa mataifa, ijapokuwa hawakuwa wakiufuatilia uadilifu,[a] waliufikia uadilifu, uadilifu unaotokana na imani;[b] **31** lakini Israeli, ijapokuwa alikuwa akiifuatilia sheria ya uadilifu, hakuifikia sheria.[c] **32** Kwa sababu gani? Kwa sababu aliifuatilia, si kwa imani, bali kama kwa matendo.[d] Walijikwaa juu ya "jiwe la kukwaza";[e] **33** kama ilivyoandikwa: "Tazama! Ninaweka katika Sayuni jiwe[f] la kukwaza na mwamba wa kuangusha,[g] lakini yeye anayemwamini hatakata tamaa."[h]

10 Akina ndugu, nia njema ya moyo wangu na dua yangu kwa Mungu kwa ajili yao, kwa kweli, ni kwa ajili ya wokovu wao.[i] **2** Kwa maana nawatolea ushahidi kwamba wana bidii[j] kwa ajili ya Mungu; lakini si kulingana na ujuzi sahihi;[k] **3** kwa maana, kwa sababu ya kukosa kujua uadilifu wa Mungu[l] bali wakitafuta kujiwekea uadilifu wao wenyewe,[m] hawakujitiisha kwa uadilifu wa Mungu.[n] **4** Kwa maana Kristo ndiye mwisho wa Sheria,[o] ili kila mtu anayeonyesha imani awe na uadilifu.[p]

5 Kwa maana Musa anaandika kwamba mtu ambaye amefanya uadilifu wa Sheria ataishi kwa huo.[q] **6** Lakini uadilifu unaotokana na imani husema kwa namna hii: "Usiseme moyoni mwako,[r] 'Ni nani atakayepanda mbinguni?'[s] yaani, kumleta Kristo[t] chini; **7** au, 'Ni nani atakayeshuka katika abiso?'[u] yaani, kumleta Kristo juu kutoka kwa wafu."[v] **8** Lakini linasema nini? "Lile neno

liko karibu nawe, katika kinywa chako mwenyewe na katika moyo wako mwenyewe”;[a] yaani, “neno”[b] la imani, ambalo sisi tunahubiri.[c] **9** Kwa maana ukitangaza waziwazi lile ‘neno lililo katika kinywa chako mwenyewe,’[d] kwamba Yesu ni Bwana,[e] na kuonyesha imani moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu,[f] utaokolewa.[g] **10** Kwa maana kwa moyo[h] mtu huonyesha imani kwa ajili ya uadilifu, lakini kwa kinywa mtu hufanya tangazo la hadharani[i] kwa ajili ya wokovu.

11 Kwa maana Andiko linasema: “Yeyote anayemwamini[j] hatakata tamaa.”[k] **12** Kwa maana hakuna tofauti kati ya Myahudi na Mgiriki,[l] kwa maana kuna Bwana yuleyule juu ya wote, aliye tajiri[m] kwa wale wote wanaomwitia. **13** Kwa maana “kila mtu anayeliitia jina la Yehova ataokolewa.”[n] **14** Hata hivyo, watawezaje kumwitia yeye ambaye hawajamwamini?[o] Nao watamwaminije yeye ambaye hawajamsikia? Nao watasikiaje bila mtu wa kuhubiri?[p] **15** Nao watahubirije isipokuwa wawe wametumwa?[q] Kama ilivyoandikwa: “Jinsi ilivyo yenye kupendeza miguu ya wale wanaotangaza habari njema ya mambo mema!”[r]

16 Hata hivyo, si wote waliotii habari njema.[s] Kwa maana Isaya anasema: “Yehova, ni nani aliyeliamini jambo ambalo limesikiwa kutoka kwetu?”[t] **17** Kwa hiyo imani hufuata jambo lililosikiwa.[u] Nalo jambo lililosikiwa ni kupitia neno kumhusu Kristo.[v] **18** Hata hivyo nauliza, Je, walikosa kusikia? Kwani, kwa kweli, “sauti yao ilifika[a] katika dunia yote, na maneno yao mpaka miisho ya dunia inayokaliwa.”[b] **19** Hata hivyo, nauliza, je, Israeli walikosa kujua?[c] Kwanza Musa anasema: “Nitawachochea ninyi kuwa na wivu kupitia lile ambalo si taifa; nitawachochea ninyi kuwa na hasira kali kupitia taifa jinga.”[d] **20** Lakini Isaya anakuwa mjasiri sana na kusema: “Wale ambao hawakuwa wakinitafuta walinipata;[e] nikajifunua kwa wale ambao hawakuwa wakiuliza juu yangu.”[f] **21** Lakini kwa habari ya Israeli yeye anasema: “Mchana kutwa nimewanyooshea mikono yangu watu wasiotii[g] na wanaojibu kwa ujeuri.”[h]

11 Basi, nauliza, Je, Mungu aliwakataa watu wake?[i] Hilo lisitendeke kamwe! Kwa maana mimi pia ni Mwisraeli,[j] wa uzao wa Abrahamu, wa kabila la Benyamini.[k] **2** Mungu hakuwakataa watu wake, aliowatambua kwanza.[l] Je, hamjui linavyosema Andiko kumhusu Eliya, anapomwomba Mungu dhidi ya Israeli?[m] **3** “Yehova, wamewaua manabii wako, wamezibomoa madhabahu zako, nami peke yangu nimebaki, nao wanaitafuta nafsi yangu.”[n] **4** Lakini, neno la Mungu[o] linamwambia nini? “Nimebakiza watu elfu saba kwa ajili yangu mwenyewe, watu ambao hawakumpigia Baali goti.”[p] **5** Basi, kwa njia hiyo katika majira ya sasa kumetokea pia mabaki[q] kulingana na kuchaguliwa[r] ambako kunatokana na fadhili zisizostahiliwa. **6** Basi ikiwa ni kwa fadhili zisizostahiliwa,[s] si

SURA 10
a Kum 30:14; Yoh 6:45; Mdo 16:14
b Lu 8:15; 2Ko 5:19
c 2Ti 4:2
d 1Ko 9:16
e Mdo 16:31
f Mdo 3:15; Ro 4:24; 1Pe 1:21
g Mt 10:32
h 1Nya 28:9; 2Th 3:5
i 2Ko 4:13; Ebr 13:15
j Yer 17:7
k Isa 28:16; Ro 9:33
l Mdo 15:9; Ga 3:28; Efe 2:14
m 1Ti 6:17
n Yoe 2:32; Sef 3:9; Mdo 2:21
o Ebr 11:6
p Lu 19:40
q Mt 28:20
r Isa 52:7; Nah 1:15; Efe 6:15
s 2Th 1:8; Ebr 4:2; 1Pe 4:17
t Isa 53:1; Yoh 12:38
u Yoh 4:42; Yoh 17:20
v Ga 3:2

Safu ya 2
a Mt 24:14; Mdo 1:8
b Zb 19:4
c Mt 10:5; Mdo 2:14
d Kum 32:21
e Ro 9:30
f Isa 65:1
g Yer 11:8; Zek 7:12
h Isa 65:2

SURA 11
i 1Sa 12:22; Yer 31:37; Amo 9:8
j Mdo 22:3; 2Ko 11:22
k Flp 3:5
l Kut 19:5; Zb 94:14
m 1Fa 19:10
n 1Fa 19:2; 1Fa 19:14
o Mdo 7:38
p 1Fa 19:18
q Yer 3:14; Ro 9:27
r Ro 9:11
s Efe 1:7; Efe 2:8

kwa sababu ya matendo[a] tena;
kama sivyo, fadhili zisizostahiliwa haziwi tena fadhili zisizostahiliwa.[b]
7 Tuseme nini, basi? Jambo
lilelile ambalo Israeli anatafuta kwa bidii yeye hakulipata,[c] lakini wale waliochaguliwa[d] walilipata. Wale wengine hisia zao zilifanywa kuwa nzito;[e]
8 kama ilivyoandikwa: "Mungu amewapa roho ya usingizi mzito,[f] macho ili wasione na masikio ili wasisikie, mpaka leo hii."[g] **9** Pia, Daudi anasema:
"Meza yao na iwe kwao mnaso na mtego na kikwazo na malipo;[h] **10** macho yao na yatiwe giza ili yasione, na sikuzote wauinamishe mgongo wao."[i]
11 Kwa hiyo nauliza, Je, wa-
lijikwaa hivi kwamba wakaanguka[j] kabisa? Hilo lisitendeke kamwe! Lakini kwa kujikwaa[k] kwao kuna wokovu kwa watu wa mataifa,[l] kuwachochea wao kuwa na wivu.[m] **12** Sasa ikiwa kujikwaa kwao humaanisha utajiri kwa ulimwengu, na kupungua kwao humaanisha utajiri kwa watu wa mataifa,[n] hesabu[o] yao kamili itamaanisha hivyo hata zaidi!
13 Sasa nasema nanyi mlio
watu wa mataifa. Kwa maana kama nilivyo, kwa kweli, mtume[p] kwa mataifa,[q] naitukuza[r] huduma[s] yangu, **14** ili labda
kwa njia yoyote ile niwachochee kuwa na wivu wale ambao ni mwili wangu mwenyewe na kuokoa[t] baadhi yao kutoka katikati yao.[u] **15** Kwa maana ikiwa kutupwa kwao[v] humaanisha upatanisho[w] kwa ulimwengu, kupokewa kwao kutamaanisha nini isipokuwa uzima kutoka kwa wafu? **16** Zaidi, ikiwa se-

SURA 11
a Ga 2:16
Efe 2:9
b Ga 5:4
c Yoh 1:11
Ro 9:31
d Yoh 1:12
Ro 11:28
e 2Ko 3:14
f Isa 29:10
g Kum 29:4
Yer 5:21
h Zb 69:22
i Zb 69:23
j 1Ko 10:8
Ebr 4:11
k Ga 6:1
l Ro 11:19
m Kum 32:21
Ro 10:19
n Ro 9:23
Kol 1:27
o Ro 11:25
Ufu 7:4
p 1Ko 9:1
1Ko 15:9
q Mdo 9:15
Ga 1:16
Efe 3:8
r Flp 1:12
2Ti 4:5
s Mdo 28:31
Kol 1:23
1Ti 1:12
t 1Ko 9:22
1Ti 4:16
u Ro 9:3
v Mt 21:43
Ebr 8:13
w Ro 5:11
2Ko 5:19

Safu ya 2
a Hes 15:21
Ne 10:37
Eze 44:30
b Law 11:44
1Pe 1:16
c Efe 2:11
Efe 2:14
d Amu 9:9
e Yer 11:16
f 1Ko 10:12
g Isa 37:31
h Isa 60:21
Ebr 2:11
i Yoh 15:6
j Mdo 15:14
k Mt 21:43
Ebr 3:19
Ebr 11:6
l Ga 3:11
Efe 2:8
m Ro 12:16
n Flp 2:12
o Yoh 15:2
p Kut 19:4
Lu 6:35
Ro 2:4
q Yud 5
r Mt 23:38
s 1Ko 15:2
t Mt 25:30
Mt 25:46
u Mdo 2:38
v Ro 11:17
w 2Ko 3:16
x 1Ko 4:1
Efe 3:5

hemu inayochukuliwa kuwa matunda ya kwanza[a] ni takatifu, donge liko hivyo pia; na ikiwa mzizi ni mtakatifu,[b] matawi yako hivyo pia.
17 Hata hivyo, ikiwa matawi
mengine yalikatwa lakini wewe, ujapokuwa mzeituni wa mwitu, ulipandikizwa katikati yake[c] na kuwa mshiriki wa mzizi wa unono[d] wa mzeituni,[e] **18** usi-
we ukifurahi juu ya hayo matawi. Ingawa hivyo, ikiwa unafurahi juu yake,[f] si wewe unayeuchukua mzizi,[g] bali ni mzizi unaokuchukua wewe.[h] **19** Basi,
wewe utasema: "Matawi yalikatwa[i] ili mimi nipandikizwe."[j]
20 Vema! Kwa sababu ya ukose-
fu wao wa imani[k] yalikatwa, lakini wewe umesimama kwa imani.[l] Uache kuwa na mawazo ya kujivuna,[m] bali uogope.[n]
21 Kwa maana ikiwa Mungu
hakuyaachilia matawi ya asili, vivyo hivyo hatakuacha wewe.[o]
22 Kwa hiyo, ona fadhili[p] na
ukali[q] wa Mungu. Kuna ukali kuwaelekea wale walioanguka,[r] lakini kuna fadhili za Mungu kukuelekea wewe, ila tu ukae[s] katika fadhili zake; kama sivyo, wewe pia utakatwa.[t] **23** Wao
pia, ikiwa hawatadumu katika ukosefu wao wa imani, watapandikizwa;[u] kwa maana Mungu anaweza kuwapandikiza tena.
24 Kwa maana ikiwa wewe uli-
katwa kutoka kwenye mzeituni ulio wa asili ya mwituni na kupandikizwa[v] kinyume cha asili katika mzeituni wa bustanini, si afadhali zaidi kwamba hawa walio wa asili wapandikizwe katika mzeituni wao wenyewe![w]
25 Kwa maana sitaki ninyi,
akina ndugu, mkose kuijua siri hii takatifu,[x] kusudi msiwe

wenye busara machoni penu
wenyewe: kwamba, kwa sehe-
mu, kumekuwa na kutiwa uzito
kwa hisi[a] za Israeli mpaka he-
sabu[b] kamili ya watu wa mata-
ifa iwe imeingia,[c] **26** na kwa
namna hii Israeli[d] wote wata-
okolewa. Kama ilivyoandikwa:
"Mkombozi atatoka katika Sa-
yuni[e] na kuondolea mbali ma-
zoea ya kutomwogopa Mungu
kutoka katika Yakobo.[f] **27** Na
hili ndilo agano kwa upande
wangu pamoja nao,[g] nitaka-
poondolea mbali dhambi zao."[h]
28 Ni kweli, kuhusiana na ha-
bari njema wao ni adui kwa
ajili yenu,[i] lakini kuhusiana
na kuchagua kwa Mungu wao
ni wapendwa kwa ajili ya ma-
babu zao.[j] **29** Kwa maana za-
wadi na mwito wa Mungu si
mambo ambayo yeye atajutia.[k]
30 Kwa maana kama vile ninyi
wakati mmoja mlivyokuwa ha-
mtii[l] Mungu lakini sasa mmeo-
nyeshwa rehema[m] kwa sababu
ya kutotii kwao,[n] **31** ndivyo
pia hawa sasa wamekuwa wasio-
tii ikitokeza rehema kwenu,[o] ili
wao wenyewe pia waonyeshwe
rehema sasa. **32** Kwa maana
Mungu amewafunga wote pa-
moja katika kutotii,[p] ili awao-
nyeshe wao wote rehema.[q]

33 Lo! Jinsi kilivyo kina cha
utajiri[r] wa Mungu na hekima[s]
na ujuzi![t] Jinsi hukumu[u] zake
zisivyochunguzika na njia zake
zisivyotafutika! **34** Kwa maa-
na "ni nani amekuja kuijua akili[v]
ya Yehova, au ni nani amekuwa
mshauri wake?"[w] **35** Au,
"Ni nani amempa yeye kwanza,
hivi kwamba iwe lazima arudi-
shiwe?"[x] **36** Kwa sababu vitu
vyote ni kutoka kwake na kwa
yeye na kwa ajili yake.[y] Kwake

SURA 11

a Ro 11:7
2Ko 3:14
b Ro 11:12
Ufu 7:4
c Ufu 7:3
d Ro 2:29
Ro 9:6
Ga 3:29
Ga 6:16
e Zb 14:7
f Isa 59:20
g Isa 59:21
h Isa 27:9
Yer 31:33
Ebr 8:8
i Ebr 4:6
j Kum 10:15
k Hes 23:19
l Efe 2:2
Efe 2:12
m Mdo 15:9
n Mdo 7:51
Ebr 3:8
o Kol 1:22
p Ro 3:9
q 1Ti 1:16
1Ti 2:4
Ebr 4:16
r Ro 2:4
Ro 9:23
s Met 2:6
Met 3:19
t Zb 139:6
u Zb 36:6
v 1Ko 2:16
w Isa 40:13
Da 4:35
x Ayu 41:11
y 1Ko 8:6

Safu ya 2

a Ga 1:5
Ufu 4:11

SURA 12

b Zb 110:3
1Ko 6:20
c Ebr 13:13
d Ro 6:13
e 2Ko 7:1
1Pe 1:15
f Law 22:19
g Flp 3:3
Ebr 9:14
h 2Ti 1:7
i 1Pe 1:14
j Ro 7:25
Efe 4:23
k 1Ti 4:15
l 1Th 4:3
Ufu 4:11
m Met 16:18
1Ko 4:6
Ga 6:3
Efe 4:2
1Pe 5:5
n Tit 2:6
1Pe 4:7
o Efe 4:7
p Efe 2:8
q 1Ko 12:12
r Kol 3:15
s 1Ko 12:25
Efe 4:25
t 1Ko 12:4
Efe 3:7
u 1Pe 4:10

yeye na kuwe na utukufu mile-
le.[a] Amina.

12 Kwa sababu hiyo nawa-
sihi ninyi kwa huruma
za Mungu, akina ndugu, mtoe
miili[b] yenu iwe dhabihu[c] iliyo
hai,[d] takatifu,[e] yenye kukubali-
ka kwa Mungu,[f] utumishi mta-
katifu[g] pamoja na nguvu zenu
za kufikiri.[h] **2** Na acheni ku-
fanyizwa[i] kulingana na mfumo
huu wa mambo, bali mgeuzwe
kwa kufanya upya akili yenu,[j] ili
mjihakikishie wenyewe[k] mape-
nzi[l] ya Mungu yaliyo mema na
yenye kukubalika na makami-
lifu.

3 Kwa maana kupitia fadhi-
li zisizostahiliwa nilizopewa na-
mwambia kila mtu hapo kati
yenu asijifikirie mwenyewe zai-
di kuliko ilivyo lazima kufikiri;[m]
bali kufikiri ili awe na akili ti-
mamu,[n] kila mmoja kama Mu-
ngu alivyomgawia kipimo[o] cha
imani.[p] **4** Kwa maana kama
vile tulivyo na viungo vingi ka-
tika mwili mmoja,[q] lakini viu-
ngo hivyo havifanyi kazi ilei-
le, **5** ndivyo sisi, ingawa tuko
wengi, ni mwili mmoja[r] kati-
ka muungano na Kristo, lakini
viungo ambavyo kila kimoja ni
cha kile kingine.[s] **6** Basi, kwa
kuwa tuna zawadi zinazotofau-
tiana[t] kulingana na fadhili zi-
sizostahiliwa[u] tulizopewa, kama
ni unabii, na tutoe unabii ku-
lingana na imani tuliyogawiwa;
7 au ni huduma, na tuwe kati-
ka huduma[v] hii; au yeye anaye-
fundisha,[w] na awe katika kufu-
ndisha[x] kwake; **8** au yeye ana-
yehimiza, na awe katika kuhi-
miza[y] kwake; yeye anayegawa,
na afanye hivyo kwa ukarimu;[z]

v 1Pe 4:11; w Ga 6:6; x 1Ti 5:17; y 2Ti 4:2; z Kum 15:11; Met 11:25; 2Ko 8:2.

yeye anayesimamia,[a] na afanye
hivyo kwa bidii ya kweli; yeye
anayeonyesha rehema,[b] na afa-
nye hivyo kwa uchangamfu.
9 Upendo[c] wenu na uwe bila
unafiki.[d] Chukieni maovu,[e] shi-
kamaneni na mema.[f] **10** Kati-
ka upendo wa kindugu[g] iweni
na upendo mwororo kwa mtu na
mwenzake. Katika kuonyesha-
na heshima[h] iweni wa kwanza.
11 Msiwe wavivu katika kazi
zenu.[i] Wakeni roho.[j] Mtumikie-
ni Yehova.[k] **12** Shangilieni ka-
tika tumaini.[l] Vumilieni chini
ya dhiki.[m] Dumuni katika sala.[n]
13 Shirikini pamoja na watakatifu kulingana na mahitaji yao.[o] Fuateni mwendo wa ukaribishaji-wageni.[p] **14** Endeleeni kuwabariki wale wanaowatesa;[q] muwe mkibariki[r] wala msiwe mkilaani.[s] **15** Shangilieni pamoja na watu wanaoshangilia;[t] lieni pamoja na watu wanaolia.
16 Mwafikirie wengine kama vile mnavyojifikiria wenyewe;[u] msiwe mkikaza akili juu ya mambo makuu,[v] bali mwongozwe na mambo ya hali ya chini.[w] Msiwe wenye busara machoni penu wenyewe.[x]

17 Msimlipe yeyote uovu
kwa uovu.[y] Fanyeni mambo
mema machoni pa watu wote.
18 Ikiwezekana, kwa kadiri
inavyowategemea ninyi, iweni
wenye kufanya amani[z] na watu
wote. **19** Wapendwa, msijili-
pizie kisasi[a] wenyewe bali iachi-
eni nafasi ghadhabu;[b] kwa maa-
na imeandikwa: "Kisasi ni cha-
ngu; mimi nitalipa, asema Yeho-
va."[c] **20** Lakini, "ikiwa adui
yako ana njaa, mlishe; ikiwa ana
kiu, mpe kitu anywe;[d] kwa maa-
na kwa kufanya hivyo utaku-
sanya makaa yenye moto juu ya
kichwa chake."[a] **21** Usiache
ushindwe na uovu, bali endelea
kuushinda uovu kwa wema.[b]

13 Kila nafsi na ijitiishe[c]
kwa mamlaka zilizo ku-
bwa,[d] kwa maana hakuna ma-
mlaka[e] isipokuwa kwa njia ya
Mungu;[f] mamlaka zilizopo zime-
simamishwa na Mungu[g] katika
vyeo vyao vya kadiri.[h] **2** Kwa
hiyo yeye anayepinga mamla-
ka amechukua msimamo kupi-
ngana na mpango wa Mungu;
wale ambao wamechukua msi-
mamo kupingana nao watapo-
kea hukumu juu yao wenye-
we.[i] **3** Kwa maana wale wana-
otawala ni kitu cha kuogope-
sha, si kwa kitendo chema, bali
kwa kibaya.[j] Basi, je, unataka
usiogope hiyo mamlaka? Ende-
lea kufanya mema,[k] nayo itaku-
sifu wewe; **4** kwa maana hiyo
ni mhudumu wa Mungu kwa-
ko kwa faida yako.[l] Lakini iki-
wa unafanya mabaya,[m] ogopa:
kwa maana haichukui upanga
bila kusudi; kwa maana hiyo ni
mhudumu wa Mungu, mlipiza-
kisasi[n] ili kuonyesha ghadhabu
juu ya yeye anayefanya mabaya.
5 Kwa hiyo kuna sababu ya
lazima kwenu muwe mkijitiisha, si kwa sababu ya ghadhabu hiyo tu, bali pia kwa sababu ya dhamiri[o] yenu. **6** Kwa maana hiyo ndiyo sababu mnalipa kodi pia; kwa maana wao ni watumishi[p] wa Mungu kwa watu wote wakitumikia daima kwa kusudi hili. **7** Wapeni wote haki zao, yeye anayetaka kodi, kodi;[q] yeye anayetaka ushuru, ushuru; yeye anayetaka woga, woga[r] huo; yeye anayetaka heshima, heshima[s] hiyo.

SURA 12
a 1Th 5:12 1Pe 5:2
b Efe 4:32
c 1Ko 13:4
d 1Ti 1:5 Yak 3:17 1Pe 1:22
e Zb 97:10 Met 8:13
f Zb 34:14 Ebr 1:9
g 1Th 4:9
h Flp 2:3
i Met 13:4
j Mdo 18:25
k Ro 6:22
l 1Th 1:3
m Mdo 14:22
n Flp 4:6 1Th 5:17
o Met 3:27 1Yo 3:17
p 1Pe 4:9 3Yo 8
q Mt 5:44
r Lu 6:28 1Ko 4:12
s Yak 3:9
t Lu 1:58
u Mt 22:39 1Pe 3:8
v Mk 10:42 Lu 22:24
w Lu 14:10 Yoh 13:14 Efe 4:2 Flp 2:3
x Ayu 37:24 Met 3:7 Yak 3:13
y 1Th 5:15 1Pe 2:23 1Pe 3:9
z 2Ti 2:24 Ebr 12:14 Yak 3:18
a Ebr 10:30
b Mt 5:39
c Law 19:18 Kum 32:35 Zb 99:8 Nah 1:2 Ebr 10:30
d Met 25:21

Safu ya 2
a Met 25:22
b Kut 23:4 Mt 5:44 Lu 6:27

SURA 13
c Tit 3:1
d 1Pe 2:13
e Lu 4:6 Ufu 13:4
f Yoh 19:11
g Mt 22:21 Mdo 5:29 1Ko 11:3
h Kum 32:8 Mdo 17:26
i Mhu 8:4
j 1Pe 2:14
k 1Pe 3:13
l Ebr 13:21
m Zb 34:16
n Isa 10:5 Isa 45:1

o 1Pe 2:19; 1Pe 3:16; p Ro 15:27; q Mt 22:21; Mk 12:17; Lu 20:25; r Met 24:21; s 1Pe 2:13; 1Pe 2:17.

8 Msiwe na deni la hata jambo moja la mtu yeyote,[a] isipokuwa kupendana;[b] kwa maana yeye anayempenda mwanadamu mwenzake ameitimiza sheria.[c] **9** Kwa maana sheria zinazosema, "Usifanye uzinzi,[d] Usiue,[e] Usiibe,[f] Usitamani,"[g] na amri nyingine yoyote iliyoko, zimejumlishwa katika neno hili, yaani, "Mpende jirani yako kama wewe mwenyewe."[h] **10** Upendo[i] haumfanyii uovu jirani ya mtu;[j] kwa hiyo upendo ndio utimizo wa sheria.[k]

11 Fanyeni hivi, pia, kwa sababu mnayajua majira, kwamba tayari ni saa ya ninyi kuamka[l] kutoka katika usingizi, kwa maana sasa wokovu wetu uko karibu zaidi kuliko wakati tulipokuwa waamini.[m] **12** Usiku umesonga sana; mchana[n] umekaribia. Kwa hiyo na tuyaondoe matendo ya giza[o] na tuvae silaha[p] za nuru. **13** Kama katika wakati wa mchana na tujiendeshe kwa adabu,[q] si katika karamu za kupindukia na vipindi vya kulewa,[r] si katika ngono isiyo halali na mwenendo mpotovu,[s] si katika mizozo[t] na wivu. **14** Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo,[u] na msiwe mkipanga kimbele kwa ajili ya tamaa za mwili.[v]

14 Mkaribisheni mtu aliye na udhaifu[w] katika imani yake, lakini msifanye maamuzi juu ya maswali ya ndani.[x] **2** Mtu mmoja ana imani ya kula kila kitu,[y] lakini mtu aliye dhaifu hula mboga za majani. **3** Yeye anayekula asimdharau yeye asiyekula,[z] na yeye asiyekula asimhukumu yeye anayekula, kwa maana Mungu amemkaribisha huyo. **4** Wewe ni nani ili umhukumu mtumishi wa nyumbani wa mwingine?[a] Kwa bwana wake mwenyewe yeye husimama au kuanguka.[b] Kwa kweli, atasimamishwa, kwa maana Yehova anaweza kumsimamisha.[c]

5 Mtu mmoja anahukumu siku moja kuwa juu ya nyingine;[d] mtu mwingine anahukumu siku moja kuwa kama nyingine zote;[e] kila mtu na asadikishwe kikamili katika akili yake mwenyewe. **6** Yeye anayeishika siku huishika kwa ajili ya Yehova. Pia, yeye anayekula, anakula kwa ajili ya Yehova,[f] kwa maana yeye humshukuru Mungu;[g] na yeye asiyekula hali chakula kwa ajili ya Yehova,[h] na bado yeye humshukuru Mungu.[i] **7** Kwa kweli, hakuna hata mmoja wetu anayeishi kwa ajili yake mwenyewe tu,[j] na hakuna yeyote anayekufa kwa ajili yake mwenyewe tu; **8** kwa maana tukiishi, tunaishi kwa ajili ya Yehova,[k] na tukifa, tunakufa kwa ajili ya Yehova.[l] Kwa hiyo tukiishi na tukifa, sisi ni wa Yehova.[m] **9** Kwa maana kwa kusudi hili Kristo alikufa na kuwa hai tena,[n] ili awe Bwana juu ya waliokufa[o] na walio hai[p] pia.

10 Lakini kwa nini wewe unamhukumu ndugu yako?[q] Au kwa nini wewe pia unamdharau ndugu yako? Kwa maana sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu[r] cha Mungu; **11** kwa maana imeandikwa: "'Kama ninavyoishi,' asema Yehova,[s] 'kila goti litapigwa mbele zangu, na kila ulimi utakiri waziwazi kwa Mungu.'"[t] **12** Hivyo, basi, kila mmoja wetu ata-

SURA 13

a Zb 37:21
b Kol 3:14
1Ti 1:5
1Yo 4:11
c Ga 5:14
Yak 2:8
d Kut 20:14
Mal 3:5
Mt 5:28
Mt 19:18
1Ko 6:9
e Mwa 9:6
Kum 5:17
Met 6:17
f Kut 20:15
g Kut 20:17
h Law 19:18
Mt 19:19
Mt 22:39
Lu 10:36
i 1Ko 13:4
j Lu 6:31
2Ti 2:24
k Mt 22:40
l Lu 21:36
1Ko 15:34
1Th 5:6
m Isa 56:1
n Efe 4:30
o Efe 5:11
p 2Ko 6:7
Efe 6:11
1Th 5:8
q 1Pe 2:12
r 1Pe 4:3
s Met 21:27
Efe 4:19
t 2Ko 12:20
Tit 3:9
u 1Ko 11:1
Ga 3:27
Efe 4:24
v Ga 5:16

SURA 14

w Ro 15:1
1Ko 8:11
1Th 5:14
x 1Ko 8:7
y Mwa 9:3
z Kol 2:16

Safu ya 2

a Mt 7:1
Yak 4:12
b 1Ko 4:4
c Yer 35:19
d Ga 4:10
e Kol 2:16
f Zb 92:1
g Mt 15:36
1Ti 4:4
h Law 11:8
Yer 36:9
i 1Ko 10:31
j 1Ko 6:19
k Zb 146:2
Ga 2:19
1Pe 4:2
l Est 4:16
Zb 116:15
m 1Th 4:14
n Yoh 12:24
o 1Th 5:10
Ufu 1:18
p Mdo 10:36
q Lu 6:37
Ro 14:4
r Mdo 10:42
Mdo 17:31
2Ko 5:10
s Isa 49:18
t Isa 45:23

toa hesabu kwa Mungu kwa ajili yake mwenyewe.[a]

13 Kwa hiyo sisi na tusiwe tukihukumiana[b] tena, bali badala yake fanyeni hili kuwa uamuzi[c] wenu, kutokuweka mbele ya ndugu[d] kikwazo[e] au sababu ya kujikwaa. **14** Najua nami nasadikishwa katika Bwana Yesu kwamba hakuna kitu ambacho ndani yake chenyewe ni najisi;[f] ni pale tu ambapo mtu anakiona kitu kuwa najisi, kwake yeye hicho huwa najisi.[g] **15** Kwa maana ikiwa ndugu yako anahuzunishwa kwa sababu ya chakula, wewe hutembei tena kupatana na upendo.[h] Kwa chakula chako usimwangamize yule ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake.[i] **16** Kwa hiyo, msiache msemwe vibaya kwa mema mnayofanya. **17** Kwa maana ufalme wa Mungu[j] haumaanishi kula na kunywa,[k] bali unamaanisha uadilifu[l] na amani[m] na shangwe[n] pamoja na roho takatifu. **18** Kwa maana yeye ambaye kwa habari hii anamtumikia Kristo anakubalika kwa Mungu naye ana kibali cha wanadamu.[o]

19 Hivyo, basi, na tufuatilie mambo yanayofanya kuwe na amani[p] na mambo ambayo ni ya kujengana.[q] **20** Acheni kuibomoa kazi ya Mungu kwa ajili ya chakula[r] tu. Ni kweli, vitu vyote ni safi, lakini ni jambo baya kwa mtu ambaye hula kukiwa na hali ya kukwaza.[s] **21** Ni vema kutokula nyama au kunywa divai au kufanya jambo lolote ambalo ndugu yako anakwazika juu yake.[t] **22** Imani uliyo nayo, uwe nayo kupatana na wewe mwenyewe machoni pa Mungu.[u] Mwenye furaha ni mtu asiyejitia mwenyewe hukumuni kwa yale anayokubali. **23** Lakini ikiwa ana shaka, yeye akila tayari atakuwa amehukumiwa kuwa mwenye hatia,[a] kwa sababu hali kwa imani. Kwa kweli, kila kitu ambacho hakitokani na imani ni dhambi.[b]

15 Ingawa hivyo, sisi tulio na nguvu tunapaswa kuchukua udhaifu wa wale wasio na nguvu,[c] na tusiwe tukijipendeza wenyewe.[d] **2** Kila mmoja wetu na ampendeze jirani yake katika yaliyo mema kwa ajili ya kujengwa kwake.[e] **3** Kwa maana hata Kristo hakujipendeza mwenyewe;[f] bali kama ilivyoandikwa: "Shutuma za wale waliokuwa wanakushutumu zimeniangukia."[g] **4** Kwa maana mambo yote yaliyoandikwa zamani yaliandikwa[h] ili kutufundisha[i] sisi, ili kupitia uvumilivu[j] wetu na kupitia faraja[k] kutokana na Maandiko tuwe na tumaini.[l] **5** Sasa Mungu anayetoa uvumilivu na faraja na awawezeshe ninyi kati yenu wenyewe kuwa na mtazamo uleule wa akili[m] ambao Kristo Yesu alikuwa nao, **6** ili kwa umoja[n] na kwa kinywa kimoja mpate kumtukuza Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo.

7 Kwa hiyo mkaribishane,[o] kama vile Kristo pia alivyotukaribisha sisi,[p] kwa kusudi la kumpa Mungu utukufu. **8** Kwa maana nasema kwamba kwa kweli Kristo alikuwa mhudumu[q] wa wale waliotahiriwa[r] kwa ajili ya ukweli[s] wa Mungu, ili kuthibitisha ahadi[t] ambazo Yeye aliwapa mababu zao, **9** na kwamba mataifa[u] yamtukuze Mungu kwa

SURA 14

a Mhu 12:14
Mt 12:36
2Ko 5:10
1Pe 4:5
b Mt 7:1
c Flp 1:10
d 1Yo 2:10
e Mt 17:27
Mt 18:6
1Ko 8:9
1Ko 10:32
f Mt 15:11
Mdo 10:15
1Ti 4:4
g Tit 1:15
h Efe 5:2
i 1Ko 8:11
j Mt 6:33
Lu 17:20
k 1Ko 8:8
l 2Pe 3:13
m Yoh 14:27
n Mt 25:21
o 2Ko 8:21
p Mt 5:9
Ro 12:18
q 1Ko 14:12
Ebr 10:24
r Ro 14:3
1Ko 8:11
s 1Ko 8:9
t Ro 14:13
1Ko 8:13
1Ko 10:24
u 1Ko 10:23

Safu ya 2

a Tit 1:15
b Yak 4:17

SURA 15

c Ro 14:1
Ga 6:1
Ga 6:2
1Th 5:14
d 1Ko 10:24
e 1Ko 9:22
Flp 2:4
f Mk 10:45
Yoh 5:30
Ga 1:4
g Zb 69:9
h Ro 4:23
1Ko 10:11
i 2Ti 3:16
2Pe 1:19
j Ro 5:4
k Zb 119:50
l 1Ko 9:10
Ebr 3:6
1Pe 1:10
m Flp 2:5
n 1Ko 1:10
2Ko 13:11
Flp 2:2
1Pe 3:8
o Flm 17
p Yoh 6:37
q Mt 20:28
r Mt 15:24
Yoh 1:11
s Mik 7:20
t Mwa 22:18
Zb 89:3
u Ro 3:29

ajili ya rehema[a] yake. Kama ilivyoandikwa: "Ndiyo sababu nitakukiri wewe waziwazi kati
ya mataifa nami nitalipigia jina
lako muziki."[b] **10** Naye anasema tena: "Furahini, enyi mataifa, pamoja na watu wake."[c]
11 Na tena: "Msifuni Yehova,
enyi mataifa yote, na vikundi
vyote vya watu vimsifu yeye."[d]
12 Na tena Isaya anasema: "Patakuwa na mzizi wa Yese,[e] na patakuwa na mmoja ambaye atasimama ili kutawala mataifa;[f] na
mataifa yatamtumainia yeye."[g]
13 Mungu anayetoa tumaini na
awajaze ninyi shangwe yote na
amani kwa kuamini kwenu, ili
mzidi katika tumaini kwa nguvu
za roho takatifu.[h]

14 Sasa mimi mwenyewe pia
ninasadikishwa juu yenu, ndugu zangu, kwamba ninyi wenyewe mmejaa wema pia, kwa
kuwa mmejawa na ujuzi[i] wote,
na kwamba mnaweza pia kuonyana.[j] **15** Hata hivyo, ninawaandikia ninyi kwa kusema
waziwazi zaidi juu ya mambo fulani, kana kwamba ninawakumbusha[k] ninyi tena, kwa sababu ya fadhili zisizostahiliwa nilizopewa kutoka kwa Mungu[l]
16 ili niwe mtumishi wa watu
wote wa Kristo Yesu kwa mataifa,[m] nikifanya kazi takatifu ya
habari njema[n] ya Mungu, ili toleo,[o] yaani, mataifa haya, likubalike,[p] likiwa limetakaswa kwa
roho takatifu.[q]

17 Kwa hiyo nina sababu ya
kufurahi katika Kristo Yesu[r]
kwa habari ya mambo yanayohusiana na Mungu.[s] **18** Kwa maana sitathubutu kusema jambo
moja ikiwa hilo si kati ya mambo
yale ambayo Kristo alifanya kupitia mimi[t] ili mataifa yawe ye-

SURA 15

a Ro 9:23
b 2Sa 22:50
Zb 18:49
c Kum 32:43
d Zb 117:1
e Isa 11:1
Ufu 5:5
f Mwa 49:10
g Isa 11:10
Mt 12:21
h Isa 40:31
Ebr 6:11
i 1Ko 8:7
Flp 1:9
2Pe 1:12
1Yo 2:21
j 2Th 3:15
k 2Pe 1:13
l Ro 12:3
Ga 1:15
Efe 3:7
m Ro 11:13
Ga 2:7
Ga 2:8
n Mt 4:23
Mk 1:1
Mdo 20:24
Efe 6:15
Ufu 14:6
o Flp 2:17
p Ro 12:1
q 2Ko 3:3
r Flp 3:3
s Ebr 2:17
Ebr 5:1
t Mt 28:20
2Ko 3:5

Safu ya 2

a Ro 16:26
b 1Ko 2:4
2Ko 13:3
c Mdo 15:12
2Ko 12:12
d Mt 10:23
e Mdo 21:19
2Ko 10:13
f 2Ko 10:15
g Isa 52:15
h Ro 1:13
i Mdo 19:21
j Ro 15:28
k Mdo 15:3
1Ko 16:6
l Mdo 11:29
Mdo 19:21
Mdo 20:22
Mdo 24:17
m 2Ko 9:2
n 1Ko 16:1
2Ko 8:4
2Ko 9:12
o Ro 11:12

nye utiifu,[a] kwa njia ya neno[b]
na tendo langu, **19** kwa nguvu za ishara na mambo ya ajabu,[c] kwa nguvu za roho takatifu; hivi kwamba kutoka Yerusalemu na kuzunguka[d] mpaka
Ilirikamu nimehubiri kikamili
habari njema juu ya Kristo.[e]
20 Kwa kweli, katika njia hii,
nilikusudia kwamba nisitangaze habari njema mahali ambapo
Kristo tayari alikuwa amekwisha kutajwa jina, ili nisiwe nikijenga juu ya msingi wa mtu mwingine;[f] **21** bali, kama ilivyoandikwa: "Wale ambao hawajatangaziwa juu yake wataona, na
wale ambao hawajasikia wataelewa."[g]

22 Kwa hiyo pia nilizuiwa
mara nyingi nisiwafikie ninyi.[h]
23 Lakini sasa kwa kuwa sina
tena eneo lisiloguswa katika
maeneo haya, na kwa miaka kadhaa nikiwa nimetamani kuwafikia ninyi[i] **24** wakati nitakapokuwa nimeenda Uhispania,[j] natumaini, zaidi ya yote,
nitakapokuwa safarini kwenda huko, niwaangalie ninyi
kidogo nanyi mnisindikize[k] kidogo kwenda huko baada ya
mimi kutosheka kwa kiasi fulani na ushirika wenu. **25** Lakini sasa nakaribia kusafiri kwenda Yerusalemu ili kuwahudumia watakatifu.[l] **26** Kwa maana wale walio katika Makedonia
na Akaya[m] wamependezwa kushiriki vitu vyao kwa kuwatolea mchango[n] fulani walio maskini kati ya watakatifu katika Yerusalemu. **27** Kweli, wamependezwa kufanya hivyo, na
bado walikuwa wadeni kwao;
kwa maana ikiwa mataifa wameshiriki mambo yao ya kiroho,[o] wao pia wana deni la kuwa-

hudumia hadharani kwa vitu
ambavyo ni kwa ajili ya mwi-
li.[a] **28** Kwa sababu hiyo nikiisha kumaliza hili na kuwafikishia salama tunda[b] hili, nitaondoka nikipitia kwenu kwenda Uhispania.[c] **29** Zaidi ya hayo, najua kwamba nitakapokuja kwenu nitakuja nikiwa na kipimo kamili cha baraka kutoka kwa Kristo.[d]

30 Sasa nawahimiza ninyi, akina ndugu, kupitia Bwana wetu Yesu Kristo na kupitia upendo wa roho,[e] kwamba mjikaze pamoja nami katika sala kwa Mungu kwa ajili yangu,[f] **31** ili nikombolewe[g] kutoka kwa wale wasioamini katika Yudea na kwamba huduma yangu ambayo ni kwa ajili ya Yerusalemu[h] ikubalike kwa watakatifu,[i] **32** ili nitakapofika kwenu nikiwa na shangwe kwa mapenzi ya Mungu niburudishwe[j] pamoja nanyi. **33** Mungu anayetoa amani na awe pamoja nanyi nyote.[k] Amina.

16 Nampendekeza kwenu Fibi dada yetu, ambaye ni mhudumu[l] wa kutaniko lililo katika Kenkrea,[m] **2** ili kwamba mkamkaribishe[n] katika Bwana kwa njia inayowastahili watakatifu, na kwamba mkamsaidie katika jambo lolote ambalo huenda akawahitaji ninyi,[o] kwa maana yeye mwenyewe pia alikuwa mtetezi wa wengi, ndiyo, wangu mimi mwenyewe.

3 Wapeni salamu zangu Priska na Akila[p] wafanyakazi wenzangu[q] katika Kristo Yesu, **4** ambao wamehatarisha shingo[r] zao wenyewe kwa ajili ya nafsi yangu, ambao si mimi tu bali pia makutaniko yote ya mataifa yanawashukuru;[a] **5** na salimuni kutaniko lililo katika nyumba yao.[b] Salimuni Epaineto mpendwa wangu, aliye matunda ya kwanza[c] ya Asia kwa ajili ya Kristo. **6** Salimuni Maria, ambaye amefanya kazi nyingi kwa ajili yenu. **7** Salimuni Androniko na Yunia jamaa[d] zangu na mateka wenzangu,[e] ambao ni watu maarufu kati ya mitume na ambao wamekuwa katika muungano[f] na Kristo muda mrefu zaidi ya mimi.

8 Mpeni salamu[g] zangu Ampliato mpendwa wangu katika Bwana. **9** Salimuni Urbano mfanyakazi mwenzetu katika Kristo, na Stako mpendwa wangu. **10** Salimuni[h] Apele, aliyekubaliwa katika Kristo. Salimuni wale wa nyumbani mwa Aristobulo. **11** Salimuni Herodioni aliye wa jamaa[i] yangu. Salimuni wale wa nyumbani mwa Narkiso walio katika Bwana.[j] **12** Salimuni Trifaina na Trifosa, wanawake wanaofanya kazi kwa bidii katika Bwana. Salimuni Persisi mpendwa wetu, kwa maana mwanamke huyo alifanya kazi nyingi katika Bwana. **13** Salimuni Rufo aliye mchaguliwa katika Bwana, na mama yake na yangu. **14** Salimuni Asinkrito, Flegoni, Hermesi, Patroba, Hermasi, na akina ndugu walio pamoja nao. **15** Salimuni Filologo na Yulia, Nerea na dada yake, na Olimpa, na watakatifu wote walio pamoja nao.[k] **16** Salimianeni kwa busu takatifu.[l] Makutaniko yote ya Kristo yanawasalimu ninyi.

17 Sasa nawahimiza ninyi, akina ndugu, waangalieni wale

SURA 15
a 1Ko 9:11
1Ko 9:14
Ga 6:6
Ebr 13:16
b Flp 4:17
c Ro 15:24
d Ro 1:11
e Flp 2:1
f 2Ko 1:11
Efe 6:18
Kol 4:3
1Th 5:25
g 2Th 3:2
h Ro 15:26
i 2Ko 8:4
j 1Ko 16:18
k Mk 5:34
Lu 1:79
1Ko 14:33
Flp 4:9
1Th 5:23
Ebr 13:20

SURA 16
l Mt 27:55
Lu 8:3
Mdo 2:18
m Mdo 18:18
n Flp 2:29
3Yo 8
o Ro 12:13
1Yo 3:17
p Mdo 18:2
Mdo 18:26
1Ko 16:19
2Ti 4:19
q 1Ko 3:9
Kol 4:11
r 1Yo 3:16

Safu ya 2
a Efe 5:20
b 1Ko 16:19
Kol 4:15
Flm 2
c 1Ko 16:15
d Ro 9:3
Ro 16:11
e Kol 4:10
f Yoh 17:21
Flp 1:1
g 2Ti 4:19
h Kol 4:15
i Ro 9:3
j Efe 6:21
Kol 4:7
k 1Ko 16:19
l 1Ko 16:20
2Ko 13:12
1Th 5:26
1Pe 5:14

wanaosababisha migawanyiko[a]
na kusababisha kukwazika kinyume cha fundisho[b] ambalo mmejifunza, nanyi mjiepushe nao.[c] **18** Kwa maana watu
wa namna hiyo ni watumwa, si
wa Bwana wetu Kristo, bali wa
matumbo[d] yao wenyewe; na kwa
maneno laini[e] na maneno ya ku-
sifusifu[f] wao huishawishi mioyo
ya wasio na lawama. **19** Kwa
maana utii wenu umekuja kuju-
likana na wote.[g] Kwa hiyo na-
shangilia juu yenu. Lakini nataka ninyi muwe wenye hekima[h]
kuhusu yaliyo mema, bali wasio
na hatia[i] kuhusu yaliyo maovu.[j]
20 Kwa upande wake, Mungu
anayetoa amani[k] atamponda
Shetani[l] chini ya miguu yenu
upesi. Fadhili zisizostahiliwa za
Bwana wetu Yesu na ziwe pamoja nanyi.[m]

21 Timotheo mfanyakazi
mwenzangu anawasalimu ninyi, na pia Lukio na Yasoni na
Sosipata jamaa[n] zangu.

SURA 16

a Yud 19
b Mt 7:15
Ro 6:17
c 2Th 3:6
2Th 3:14
Tit 3:10
2Yo 10
d Flp 3:19
Yud 12
e 2Pe 2:3
Yud 16
f Kol 2:4
Tit 1:10
g Ro 1:8
h Kol 1:9
i Mt 10:16
j Yer 4:22
1Ko 14:20
k Ro 15:33
l Mwa 3:15
Ebr 2:14
m 1Ko 16:23
Ufu 22:21
n Ro 9:3
Ro 16:7

Safu ya 2

a 1Ko 1:14
b Mdo 19:35
c Efe 3:20
Yud 24
d Efe 1:9
Efe 3:9
Kol 1:26
e 2Ti 1:10
f Mdo 6:7
Tit 1:3
g Ro 11:33
h Ga 1:5
i Ebr 13:21

22 Mimi, Tertio, ambaye ni-
meiandika barua hii, nawasali-
mu ninyi katika Bwana.

23 Gayo,[a] mkaribishaji wa-
ngu na wa kutaniko lote, ana-
wasalimu ninyi. Erasto msima-
mizi wa jiji[b] anawasalimu ni-
nyi, na pia Kwarto ndugu yake.
24 ——

25 Sasa kwa yeye[c] anayewe-
za kuwafanya ninyi kuwa ima-
ra kulingana na habari nje-
ma ninayotangaza na kuhubiri-
wa kwa Yesu Kristo, kwa kupa-
tana na ufunuo wa siri takatifu[d]
ambayo imewekwa katika siri
tangu nyakati za zamani za kale
26 lakini sasa imefunuliwa[e] na
kujulishwa kupitia maandiko
ya kinabii kati ya mataifa yote
kwa kupatana na amri ya Mu-
ngu anayedumu milele ili kue-
ndeleza utii kwa njia ya imani;[f]
27 kwa Mungu, mwenye heki-
ma peke yake,[g] kuwe na utuku-
fu[h] kupitia Yesu Kristo[i] milele.
Amina.

BARUA YA KWANZA KWA

WAKORINTHO

1 Paulo, aliyeitwa kuwa mtu-
me[a] wa Yesu Kristo kupi-
tia mapenzi ya Mungu,[b] na Sos-
thene[c] ndugu yetu **2** kwa ku-
taniko la Mungu lililo katika
Korintho,[d] kwenu ninyi ambao
mmetakaswa[e] katika muunga-
no na Kristo Yesu, mlioitwa
kuwa watakatifu,[f] pamoja na
wote ambao kila mahali wana-
liitia jina[g] la Bwana wetu, Yesu
Kristo, Bwana wao na wetu:[h]

3 Na muwe na fadhili zisi-
zostahiliwa[i] na amani[j] kutoka
kwa Mungu Baba yetu na Bwa-
na Yesu Kristo.[a]

4 Sikuzote ninamshukuru
Mungu kwa ajili yenu kwa saba-
bu ya fadhili zisizostahiliwa[b] za
Mungu mlizopewa katika Kri-
sto Yesu;[c] **5** kwamba katika
kila jambo mmetajirishwa[d] kati-
ka yeye, katika uwezo kamili wa
kusema na katika ujuzi kami-
li,[e] **6** kama vile ushahidi juu

SURA 1

a Mdo 9:15
Ro 1:1
1Ti 2:7
b 2Ko 1:1
Kol 1:1
c Mdo 18:17
d Mdo 18:1
e Yoh 17:19
1Ko 6:11
Ebr 2:11
Ebr 9:14
f Da 7:27
1Pe 1:15
g Mt 12:21
Mdo 4:12
h Ro 3:22
Efe 4:3
i Tit 2:11
j Hes 6:26
Flp 4:7

Safu ya 2 a 2Pe 1:2; b Yoh 1:17; c Efe 1:7; Efe 2:7; d 2Ko 8:9; Efe 3:19; e Kol 1:9.

ya Kristo[a] ulivyofanywa kuwa
imara katikati yenu, **7** ili kwa-
mba msipungukiwe katika za-
wadi[b] yoyote hata kidogo, huku
mkiungojea kwa hamu ufunuo[c]
wa Bwana wetu Yesu Kristo.
8 Yeye pia atawafanya ninyi
imara[d] mpaka mwisho, ili msi-
we na shtaka[e] lolote katika siku[f]
ya Bwana wetu Yesu Kristo.[g]
9 Mungu ni mwaminifu,[h] aliye-
waita kuingia katika ushirika[i]
pamoja na Mwana wake Yesu
Kristo Bwana wetu.

10 Sasa nawahimiza[j] ninyi,
akina ndugu, kupitia jina[k] la
Bwana wetu Yesu Kristo kwa-
mba nyote mseme kwa upata-
no,[l] na kwamba kusiwe na mi-
gawanyiko[m] katikati yenu, bali
kwamba muunganishwe vema
katika akili ileile na katika njia
ileile ya kufikiri.[n] **11** Kwa maa-
na, ndugu zangu, wale wa nyu-
mba ya Kloe walinifunulia[o] juu
yenu kwamba kuna magomba-
no kati yenu. **12** Ninalomaa-
nisha ni hili, kwamba kila mmo-
ja wenu anasema: "Mimi ni wa
Paulo," "Lakini mimi ni wa Apo-
lo,"[p] "Lakini mimi ni wa Kefa,"
"Lakini mimi ni wa Kristo."
13 Kristo amegawanyika.[q] Je,
Paulo alitundikwa mtini kwa
ajili yenu? Au je, mlibatizwa[r]
katika jina la Paulo? **14** Mimi
nashukuru kwa kuwa sikubati-
za hata mmoja wenu isipokuwa
Krispo[s] na Gayo,[t] **15** ili yeyo-
te asiseme kwamba mlibatizwa
katika jina langu. **16** Ndiyo,
niliibatiza pia nyumba ya Ste-
fana.[u] Kuhusu wale wengine, si-
jui kama nilimbatiza mwingine
yeyote. **17** Kwa maana Kristo
alinituma,[v] si kwenda kubatiza,
bali kwenda kutangaza habari
njema, si kwa maneno ya heki-
ma,[a] ili mti wa mateso wa Kristo
usifanywe kutofaa kitu.

18 Kwa maana neno juu ya
mti wa mateso ni upumba-
vu[b] kwa wale wanaoangamia,[c]
lakini kwetu sisi tunaookolewa[d]
ni nguvu za Mungu.[e] **19** Kwa
maana imeandikwa: "Nitaia-
ngamiza hekima ya watu wenye
hekima,[f] na akili ya watu we-
nye akili[g] nitaitupa kando."[h]
20 Yuko wapi mtu mwenye he-
kima? Yuko wapi mwandishi?[i]
Yuko wapi mwenye kubishania[j]
maneno wa mfumo huu wa ma-
mbo?[k] Je, Mungu hakuifanya
hekima ya ulimwengu iwe upu-
mbavu?[l] **21** Maana, kwa kuwa
katika hekima ya Mungu, uli-
mwengu kupitia hekima yake[m]
haukuja kumjua Mungu,[n] Mu-
ngu aliona vema kupitia upumba-
vu[o] wa linalohubiriwa awaokoe
wale wanaoamini.

22 Kwa maana Wayahudi
wanaomba ishara[p] na Wagiriki
wanatafuta hekima;[q] **23** laki-
ni sisi tunamhubiri Kristo aliye-
tundikwa mtini,[r] kwa Wayahu-
di ni sababu ya kujikwaa[s] lakini
kwa mataifa ni upumbavu;[t]
24 hata hivyo, kwa wale walioi-
twa, Wayahudi na Wagiriki, Kri-
sto ni nguvu[u] za Mungu na heki-
ma[v] ya Mungu. **25** Kwa saba-
bu kitu kipumbavu cha Mungu
ni chenye hekima zaidi kuliko
wanadamu, na kitu dhaifu cha
Mungu ni chenye nguvu zaidi
kuliko wanadamu.[w]

26 Kwa maana mnaona mwi-
to wake kwenu, akina ndugu,
kwamba si wengi wenye heki-
ma[x] katika njia ya kimwili wa-
lioitwa,[y] si wengi wenye ngu-
vu,[z] si wengi wa uzawa wa cheo;
27 bali Mungu alivichagua vitu
vipumbavu vya ulimwengu,[a] ili
awaaibishe watu wenye hekima;

SURA 1

a Mdo 18:5
2Ti 1:8
b Ebr 6:4
c Lu 17:30
2Th 1:7
1Pe 1:7
d Ro 14:4
1Th 3:13
2Th 3:3
e Kol 1:22
f 1Ko 4:5
1Ko 5:5
Ufu 1:10
g 1Th 5:23
h Kum 7:9
Isa 49:7
i Yoh 17:21
1Yo 1:3
j 2Th 3:6
k 2Ko 13:10
l 2Ko 13:11
Flp 2:2
m Ro 16:17
Efe 4:3
n Ro 15:5
2Ko 13:11
o Law 5:1
1Ko 5:1
p Mdo 18:24
1Ko 3:4
1Ko 3:21
q Efe 4:5
r Mdo 2:38
s Mdo 18:8
t Ro 16:23
u 1Ko 16:15
v Mdo 9:15

Safu ya 2

a 1Ko 2:1
b Mdo 17:18
1Ko 2:14
c 1Yo 2:17
d 1Ko 15:2
e Ro 1:16
f Zb 33:10
1Ko 3:19
g Yer 8:9
1Ti 6:20
h Isa 29:14
i Isa 33:18
j Mdo 17:18
k Efe 2:2
l Ayu 12:17
Ro 1:22
m Kol 2:8
n Mt 11:25
Lu 10:21
o Mdo 17:19
1Ko 2:14
1Ko 3:18
p Mt 12:38
Lu 11:29
q Mdo 17:18
r 1Ko 2:2
s Isa 8:14
t Mdo 17:32
u Mk 13:26
v 1Ko 1:30
Kol 2:3
w 2Ko 13:4
x Mdo 4:13
y Ro 8:30
z Yoh 7:48
Yak 2:5
a Lu 16:8

na Mungu alivichagua vitu dhaifu vya ulimwengu, ili aviaibishe
vitu vyenye nguvu;[a] **28** na
Mungu alivichagua vitu vinyonge vya ulimwengu na vitu vinavyodharauliwa, vitu ambavyo si
kitu,[b] ili kuvifanya viwe si kitu[c]
vitu ambavyo ni kitu **29** ili
mwili wowote usijisifu[d] machoni pa Mungu. **30** Lakini ni
kwa sababu yake kwamba ninyi
mko katika muungano na Kristo Yesu, ambaye kwetu amekuwa hekima[e] kutoka kwa Mungu, pia uadilifu[f] na utakaso[g] na
kuachiliwa huru kupitia fidia;[h]
31 ili iwe kama ilivyoandikwa:
"Yeye anayejisifu, na ajisifu katika Yehova."[i]

2 Na kwa hiyo mimi, nilipokuja kwenu, akina ndugu,
sikuja na wingi wa maneno[j] au
wa hekima nikiwatangazia siri
takatifu[k] ya Mungu. **2** Kwa
maana niliamua kutojua kitu
chochote katikati yenu isipokuwa Yesu Kristo,[l] naye akiwa
ametundikwa mtini. **3** Nami
nilikuja kwenu katika udhaifu
na katika woga na kwa kutetemeka kwingi;[m] **4** na maneno yangu na mambo niliyohubiri hayakuwa kwa maneno yenye kushawishi ya hekima bali
kwa wonyesho wa roho na nguvu,[n] **5** ili imani yenu iwe, si katika hekima[o] ya wanadamu, bali
katika nguvu za Mungu.[p]

6 Basi tunasema hekima katikati ya wale ambao ni wakomavu,[q] lakini si hekima[r] ya mfumo huu wa mambo wala ile ya
watawala wa mfumo huu wa mambo,[s] ambao watakuja kuwa si
kitu.[t] **7** Bali tunasema hekima ya Mungu katika siri takatifu,[u] hekima iliyofichwa, ambayo
Mungu aliagiza kimbele kabla
ya mifumo[v] ya mambo kwa aji-

SURA 1

a Mt 11:25
b Ro 4:17
c 1Ko 2:6
d Ro 3:27
1Ko 4:7
e Yer 23:5
Ufu 5:12
f Ro 10:4
2Ko 5:21
g Yoh 17:19
Ebr 10:10
h Ro 3:24
Kol 1:14
i Yer 9:24
2Ko 10:17

SURA 2

j 1Ko 1:17
2Ko 10:10
2Ko 11:6
k Efe 3:5
Kol 2:2
l Ga 6:14
Flp 3:8
m 2Ko 10:1
Ga 4:13
n Ro 15:19
1Ko 4:20
1Th 1:5
2Pe 1:16
o Efe 1:17
p 2Ko 4:7
2Ko 6:7
q 1Ko 14:20
Efe 4:13
Ebr 5:14
r 1Ko 3:20
2Ko 1:12
1Ti 6:20
s Mt 20:25
t 1Ko 15:24
u Mwa 3:15
Ro 16:25
Efe 3:9
v Kol 1:26

Safu ya 2

a Yoh 7:48
Mdo 13:27
b 1Ko 1:18
2Ko 3:14
c Mdo 4:10
Mdo 5:30
d Isa 64:4
e Kum 29:29
Mt 16:17
Mk 4:11
Efe 3:5
2Ti 1:10
1Pe 1:12
f Yoh 14:26
1Yo 2:27
g Ro 8:26
h Ayu 11:7
Ro 11:33
Efe 3:18
i Ro 1:9
Ro 8:16
j Yoh 14:17
Ro 8:27
k 1Yo 4:3
1Yo 5:19
Ufu 16:14
l Yoh 15:26
m 1Yo 4:6
n Kol 2:8
1Ti 6:20
2Pe 1:16
o Yoh 16:13
p Met 1:23
Yoh 6:63
q Mt 16:23
r Ro 8:5

li ya utukufu wetu. **8** Hekima
hii hakuna hata mmoja wa watawala[a] wa mfumo huu wa mambo
aliyeijua,[b] kwa maana kama
wao wangaliijua hawangalimtundika mtini[c] Bwana mwenye
utukufu. **9** Lakini kama ilivyoandikwa: "Jicho halijaona
na sikio halijasikia, wala hayajawaziwa katika moyo wa mwanadamu mambo ambayo Mungu
amewatayarishia wale wanaompenda."[d] **10** Kwa maana ni
kwetu sisi Mungu ameyafunua[e]
kupitia roho[f] yake, kwa maana
roho[g] huchunguza ndani ya mambo yote, hata mambo mazito[h]
ya Mungu.

11 Kwa maana ni nani kati
ya wanadamu anayejua mambo ya mwanadamu isipokuwa roho[i] ya mwanadamu iliyo
ndani yake? Vivyo hivyo, pia,
hakuna ambaye amekuja kuyajua mambo ya Mungu, isipokuwa roho[j] ya Mungu. **12** Basi
sisi tulipokea, si roho[k] ya ulimwengu, bali roho[l] inayotoka
kwa Mungu, ili tuyajue mambo
ambayo Mungu ametupa sisi
kwa fadhili.[m] **13** Mambo hayo
tunayasema pia, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya binadamu,[n] bali kwa yale
yanayofundishwa kwa roho,[o] tunapounganisha mambo ya kiroho pamoja na maneno ya kiroho.[p]

14 Lakini mtu wa kimwili
hayapokei mambo ya roho ya
Mungu, kwa maana hayo ni upumbavu kwake; naye hawezi kuyajua,[q] kwa sababu hayo huchunguzwa kiroho. **15** Hata
hivyo, mtu wa kiroho[r] huchunguza mambo yote, lakini yeye
mwenyewe hachunguzwi[s] na

s 1Ko 4:3.

mwanadamu yeyote. **16** Kwa
maana "ni nani ameijua aki-
li ya Yehova,[a] ndipo amfundi-
she?"[b] Lakini sisi tunayo akili[c]
ya Kristo.

3 Na kwa hiyo, akina ndugu,
mimi sikuweza kusema na-
nyi kama watu wa kiroho,[d] bali
kama watu wa kimwili, kama
watoto[e] katika Kristo. **2** Nili-
walisha ninyi maziwa, si chaku-
la,[f] kwa maana mlikuwa bado
hamna nguvu za kutosha. Kwa
kweli, hata sasa hamna ngu-
vu za kutosha,[g] **3** kwa maana
bado ninyi ni wa kimwili.[h] Kwa
kuwa kuna wivu na mizozo kati
yenu,[i] je, ninyi si wa kimwili na
je, hamtembei kama wanadamu
wanavyotembea?[j] **4** Kwa ma-
ana mtu anaposema: "Mimi ni
wa Paulo," lakini mwingine ana-
sema: "Mimi ni wa Apolo,"[k] je,
ninyi si wanadamu tu?

5 Basi, Apolo[l] ni nani? Ndi-
yo, Paulo ni nani? Wahudu-
mu[m] ambao kupitia wao mli-
kuja kuwa waamini, kama vile
Bwana alivyompa kila mmoja.
6 Mimi nilipanda,[n] Apolo aka-
tia maji,[o] lakini Mungu aka-
ndelea kuikuza;[p] **7** hivi kwa-
mba yeye anayepanda si kitu[q]
wala yeye anayetia maji, bali
Mungu anayeikuza.[r] **8** Basi
yeye anayepanda na yeye ana-
yetia maji ni kitu kimoja,[s] laki-
ni kila mtu atapokea thawabu
yake mwenyewe kulingana na
kazi yake mwenyewe.[t] **9** Kwa
maana sisi ni wafanyakazi we-
nzi wa Mungu.[u] Ninyi ni shamba
la Mungu linalolimwa,[v] jengo la
Mungu.[w]

10 Kulingana na fadhili zi-
sizostahiliwa[x] za Mungu nili-
zopewa, mimi kama msimami-
zi wa ujenzi mwenye hekima
niliweka msingi,[y] lakini mtu
mwingine anajenga juu yake.
Lakini kila mmoja na aendelee
kuangalia jinsi anavyojenga juu
yake.[a] **11** Kwa maana haku-
na mtu anayeweza kuweka msi-
ngi[b] mwingine wowote kuliko
ule uliowekwa, ambao ni Yesu
Kristo.[c] **12** Basi yeyote akije-
nga juu ya msingi huo dhaha-
bu, fedha, mawe ya thamani, vi-
faa vya mbao, nyasi kavu, ma-
jani makavu, **13** kazi ya kila
mmoja itafunuliwa, kwa maana
ile siku itaifichua, kwa sababu
itafunuliwa kwa njia ya moto;[d]
na moto wenyewe utaonyesha
kazi ya kila mmoja ni ya aina
gani. **14** Kazi ya yeyote amba-
yo ameijenga juu yake ikibaki,[e]
atapokea thawabu;[f] **15** kazi
ya yeyote ikiteketea, atapata
hasara, lakini yeye mwenyewe
ataokolewa;[g] lakini, ikiwa hi-
vyo, itakuwa ni kama kupitia
katika moto.[h]

16 Je, hamjui kwamba ninyi
ni hekalu la Mungu,[i] na kwa-
mba roho ya Mungu inakaa nda-
ni yenu?[j] **17** Yeyote akiliange-
miza hekalu la Mungu, Mungu
atamwangamiza yeye;[k] kwa ma-
ana hekalu la Mungu ni takati-
fu,[l] nanyi ni[m] hekalu[n] hilo.

18 Yeyote asiwe akijishawi-
shi mwenyewe: Yeyote kati
yenu akifikiri yeye ni mwenye
hekima[o] katika mfumo huu wa
mambo, acheni awe mpumba-
vu, ili awe mwenye hekima.[p]
19 Kwa maana hekima ya uli-
mwengu huu ni upumbavu kwa
Mungu;[q] kwa maana imeandi-
kwa: "Yeye huwakamata we-
nye hekima katika ujanja[r] wao
wenyewe." **20** Na tena: "Yeho-
va anajua kwamba kufikiri kwa
watu wenye hekima ni kwa uba-
tili."[s] **21** Kwa hiyo yeyote asi-
we akijisifu katika watu; kwa

SURA 2

a Ro 11:34
b Isa 40:13
c Ro 15:5
Flp 2:5

SURA 3

d Mt 5:3
1Ko 2:15
Kol 1:9
Yud 19
e 1Ko 14:20
f Ebr 5:12
Ebr 5:14
g Ebr 5:13
h Ro 8:7
Ga 5:17
i Ro 13:13
2Ko 12:20
Ga 5:19
j 1Pe 4:3
k 1Ko 1:12
1Ko 11:18
l Mdo 18:24
m 2Ko 3:6
Kol 1:23
1Ti 1:12
n Mdo 18:4
o Mdo 18:25
Mdo 18:28
Mdo 19:1
p Isa 55:10
2Ko 9:10
q 2Ko 12:11
Ga 6:3
r Ro 9:16
2Ko 6:1
s Ga 3:28
t Ro 2:6
1Ko 4:5
Flp 2:13
Ufu 22:12
u 1Ko 3:6
v Mt 13:38
w Efe 2:22
1Pe 2:5
x 1Ko 15:10
y Ro 15:20
Ebr 6:1

Safu ya 2

a 1Pe 4:11
b Isa 28:16
1Pe 2:6
c Zb 118:22
Mt 21:42
Mdo 4:11
Efe 2:20
d Da 11:35
Zek 13:9
1Pe 1:7
1Pe 4:12
e Mt 7:25
f 1Ko 9:17
g Eze 3:19
h Yud 23
i 2Ko 6:16
Efe 2:21
1Pe 2:5
j Ro 8:9
1Ko 6:19
k Isa 54:15
2Th 1:6
l Zb 11:4
m 1Pe 2:5
n 2Ko 6:16
o Met 3:7
Lu 16:8
p Da 12:3
Da 12:10
q 1Ko 1:20
r Ayu 5:13
Lu 20:23
s Zb 94:11

maana vitu vyote ni vyenu,[a]
22 kama ni Paulo au Apolo[b] au
Kefa au ulimwengu au uzima
au kifo au mambo yaliyo hapa
sasa au mambo yatakayokuja,[c]
vitu vyote ni vyenu; **23** nanyi
ni wa Kristo;[d] naye Kristo ni wa
Mungu.[e]

4 Acheni mtu atukadirie sisi
hivyo kuwa tuko chini ya[f]
Kristo nasi ni wasimamizi-nyumba[g] wa siri takatifu[h] za Mungu. **2** Mbali na hilo, katika
hali hii, kinachoangaliwa katika wasimamizi-nyumba[i] ni mtu
kupatwa akiwa mwaminifu.[j]
3 Basi kwangu ni jambo dogo
sana kwamba ninyi au baraza
la kibinadamu mnichunguze.[k]
Hata mimi sijichunguzi mwenyewe. **4** Kwa maana sifahamu[l] kitu chochote dhidi yangu
mwenyewe. Lakini kwa hilo si-
onyeshwi kuwa mwadilifu, bali
yeye anayenichunguza ni Yeho-
va.[m] **5** Kwa hiyo msihukumu[n]
kitu chochote kabla ya waka-
ti unaofaa, mpaka Bwana aje,[o]
atakayeyaleta kwenye nuru ma-
mbo ya siri yaliyo ya giza[p] na pia
kuyafunua mashauri ya mioyo,[q]
na ndipo kila mtu atakapopata
sifa yake kutoka kwa Mungu.[r]

6 Basi, akina ndugu, mambo
haya nimeyahamisha ili kuya-
tumia juu yangu mwenyewe na
Apolo[s] kwa faida yenu, ili katika
hali yetu mjifunze kanuni: "Msi-
pite mambo yaliyoandikwa,"[t] ili
msijivune[u] mtu mmoja-mmoja
kwa kumpendelea mtu mmoja
juu ya mwingine.[v] **7** Kwa ma-
ana ni nani anayekufanya wewe
kuwa tofauti[w] na mwingine?
Kwa kweli, una nini ambacho
hukupokea?[x] Basi, ikiwa kwa
kweli ulikipokea,[y] kwa nini una-
jisifu[z] kana kwamba hukuki-
pokea?

SURA 3

a 2Ko 4:15
b 1Ko 1:12
c Ro 8:38
d Yoh 17:9
2Ko 10:7
e 1Ko 11:3

SURA 4

f Lu 1:2
2Ko 5:20
g Lu 12:42
1Ko 9:17
Kol 1:25
Tit 1:7
h Mt 13:11
Ro 16:25
i Mwa 24:2
j Mwa 39:9
Ga 3:9
Ebr 3:5
k Mt 10:17
1Pe 4:6
l Ayu 27:6
Mdo 23:1
Mdo 24:16
m Met 21:2
Ro 14:10
Ebr 4:13
n Mt 7:1
o Mal 3:2
Mt 24:3
Ufu 1:10
p Met 10:9
Mt 10:26
Lu 8:17
1Ti 5:24
q Lu 2:35
1Th 2:4
r Yoh 5:44
Ro 2:29
2Ko 10:18
s 1Ko 1:12
1Ko 3:22
t 1Ko 1:31
2Yo 9
3Yo 9
u Ro 12:3
v 2Ko 12:20
w Ro 12:6
x Yoh 3:27
Yak 1:17
y 1Pe 4:10
z Ga 6:14

Safu ya 2

a Ufu 3:17
b Ufu 20:4
Ufu 20:6
c 2Ti 2:12
Ufu 3:21
d 1Ko 15:32
e Zb 44:22
Ro 8:36
2Ko 6:9
Ufu 6:9
f Ebr 10:33
g Efe 6:12
1Pe 1:12
h 2Ko 2:16
i 1Ko 3:18
j Mt 10:16
k 2Ko 11:29
l 1Ko 10:12
m Ga 2:6
n Yoh 8:49
o Flp 4:12
p 2Ko 11:27
q Ro 8:35
r Mdo 14:19
Mdo 23:2
2Ko 11:24
s Mt 8:20
t 1Th 2:9

8 Ninyi tayari mmepata shi-
be yenu, sivyo? Ninyi tayari ni
matajiri, sivyo?[a] Mmeanza kuta-
wala mkiwa wafalme[b] bila sisi,
sivyo? Nami ningalipenda kwa-
mba muwe mmeanza kutawala
mkiwa wafalme, ili sisi pia tu-
tawale pamoja nanyi tukiwa wa-
falme.[c] **9** Kwa maana inaone-
kana kwangu kwamba Mungu
ametuweka sisi mitume mwi-
sho katika wonyesho wa ha-
dharani[d] kama watu walioweke-
wa kifo,[e] kwa sababu tumeku-
wa tamasha[f] kwa ulimwengu,
na kwa malaika,[g] na kwa wana-
damu.[h] **10** Sisi ni wapumbavu[i]
kwa sababu ya Kristo, lakini ni-
nyi ni wenye busara[j] katika Kri-
sto; sisi ni dhaifu,[k] lakini ninyi
ni wenye nguvu;[l] ninyi mna sifa
njema,[m] lakini sisi tumo kati-
ka aibu.[n] **11** Mpaka saa hii sisi
tunaendelea kupata njaa[o] na
pia kupata kiu[p] na kuvaa mava-
zi machache[q] na kupigwa[r] huku
na huku na kuwa bila makao[s]
12 na kufanya kazi ya kutaabi-
ka,[t] tukifanya kazi kwa mikono
yetu wenyewe.[u] Tunapotuka-
nwa, tunabariki;[v] tunapoteswa,
tunavumilia;[w] **13** tunapoha-
ribiwa sifa, tunasihi;[x] tumeku-
wa kama takataka ya ulimwe-
ngu, uchafu wa vitu vyote, mpa-
ka sasa.[y]

14 Ninaandika mambo haya,
si ili kuwaaibisha ninyi, bali
kuwaonya kama watoto wangu
wapendwa.[z] **15** Kwa maana
ingawa huenda mkawa na wa-
tunzaji[a] elfu kumi katika Kristo,
hakika hamna baba wengi;[b] kwa
maana katika Kristo Yesu mimi
nimekuwa baba yenu kupitia
habari njema.[c] **16** Kwa hiyo,

u Mdo 18:3; Mdo 20:34; 2Th 3:8; v Zb 109:28; Ro 12:14; 1Pe 3:9; w Mt 5:44; x 1Pe 2:23; y Omb 3:45; z 2Ko 6:13; a Ga 3:24; b 3Yo 4; c Ga 4:19; 1Th 2:11.

nawasihi ninyi, iweni waigaji
wangu.[a] **17** Ndiyo sababu ni-
namtuma Timotheo kwenu,[b]
kwa kuwa yeye ni mtoto wangu
mpendwa[c] na mwaminifu katika Bwana; naye atawakumbusha ninyi njia zangu kuhusiana na Kristo Yesu,[d] kama vile ninavyofundisha kila mahali katika kila kutaniko.

18 Wengine wamejivuna[e] kana kwamba siji kwenu. **19** Lakini nitakuja kwenu hivi karibuni, Yehova akipenda,[f] nami nitajua, si maneno ya wale ambao wanajivuna, bali nguvu zao. **20** Kwa maana ufalme wa Mungu hauko katika maneno, bali katika nguvu.[g] **21** Mnataka nini? Je, nije kwenu nikiwa na fimbo,[h] au kwa upendo na upole wa roho?[i]

5 Kwa kweli kuna habari kwamba kuna uasherati[j] katikati yenu, tena uasherati wa namna ambayo hata haimo kati ya mataifa, kwamba mwanamume fulani ana mke wa baba yake.[k] **2** Na je, ninyi mnajivuna,[l] na badala yake hamwombolezi,[m] ili mtu aliyefanya kitendo hicho aondolewe mbali kutoka kati yenu?[n] **3** Mimi kwa kweli, ijapokuwa sipo katika mwili bali nipo katika roho, tayari nimemhukumu,[o] kana kwamba nipo, mtu huyo ambaye amefanya tendo la namna hiyo, **4** kwamba katika jina la Bwana wetu Yesu, wakati mnapokuwa mmekusanyika pamoja, pia roho yangu pamoja na nguvu za Bwana wetu Yesu,[p] **5** mkamkabidhi mtu wa namna hiyo kwa Shetani[q] kwa ajili ya kuangamizwa kwa mwili, ili roho[r] iokolewe katika siku ya Bwana.[s]

6 Sababu ya kujisifu[t] kwenu si nzuri. Je, hamjui kwamba chachu kidogo huchachisha[a] donge lote?[b] **7** Ondoleeni mbali chachu ya zamani, ili muwe donge jipya,[c] kulingana na mlivyo bila chachu. Kwa maana, kwa kweli, Kristo[d] pasaka[e] yetu ametolewa dhabihu.[f] **8** Kwa hiyo na tufanye sherehe,[g] si kwa chachu[h] ya zamani, wala si kwa chachu[i] ya ubaya na uovu,[j] bali kwa keki zisizo na chachu za unyoofu na kweli.[k]

9 Katika barua yangu niliwaandikia ninyi mwache kuchangamana katika ushirika na waasherati, **10** si kumaanisha kabisa na waasherati[l] wa ulimwengu[m] huu au watu wenye pupa na wanyang'anyi au waabudu-sanamu. Ikiwa hivyo, kwa kweli ingewabidi mwondoke katika ulimwengu.[n] **11** Lakini sasa ninawaandikia ninyi mwache kuchangamana katika ushirika[o] pamoja na mtu yeyote anayeitwa ndugu ambaye ni mwasherati au mtu mwenye pupa[p] au mwabudu-sanamu au mtukanaji au mlevi[q] au mnyang'anyi, hata msile chakula pamoja na mtu wa namna hiyo. **12** Kwa maana inanihusu nini kuwahukumu wale walio nje?[r] Je, ninyi hamwahukumu wale walio ndani,[s] **13** huku Mungu akiwahukumu wale walio nje?[t] "Ondoeni yule mtu mwovu kati yenu."[u]

6 Je, yeyote kati yenu aliye na kesi[v] juu ya mwingine anathubutu kwenda mahakamani mbele ya watu wasio waadilifu,[w] na si mbele ya watakatifu?[x] **2** Au je, hamjui kwamba watakatifu watauhukumu[y] ulimwengu?[z] Na ikiwa ninyi mtauhukumu ulimwengu, je, hamstahili

SURA 4
a 1Ko 11:1 Flp 3:17 1Th 1:6
b Mdo 19:22 Flp 2:19 1Th 3:2
c 2Ti 1:2
d Lu 6:40 2Ti 1:13
e 1Ti 3:6
f Mdo 18:21 Yak 4:15
g 1Ko 2:4 1Th 1:5
h 2Ko 10:8 2Ko 13:10
i Ga 6:1

SURA 5
j Efe 5:3
k Mwa 35:22 Law 18:8 Kum 22:30
l 1Ko 4:18
m Eze 9:4 2Ko 7:9
n 1Ko 5:13 2Yo 10
o 1Ko 6:3
p Yoh 20:23
q Mdo 26:18 1Ti 1:20
r 1Ko 7:34
s 1Ko 1:8
t 1Ko 3:21 Yak 4:16

Safu ya 2
a Ga 5:9 2Ti 2:17
b Mhu 9:18 1Ko 15:33
c Ga 6:15
d 1Pe 1:19
e Yoh 1:29
f Ufu 5:12
g Kut 13:7
h Kum 16:3
i Mt 16:12
j 1Pe 4:3
k Yoh 1:17 Yoh 17:17
l Ro 1:28 1Ko 6:9 Efe 5:5
m 1Yo 2:17
n Yoh 17:15
o Hes 16:26 Ro 16:17 2Th 3:6 2Yo 10
p Efe 5:5
q Kum 21:20 1Ko 6:10 Ga 5:21 1Pe 4:3
r Mk 4:11
s 1Ko 6:5
t Mhu 12:14
u Mwa 3:24 Kum 17:7 Tit 3:10 2Yo 10

SURA 6
v Mt 18:15
w Mdo 18:17
x 1Ko 5:3 Tit 1:9 Ebr 13:17

y Lu 22:30; Ufu 20:4; z 2Pe 3:7.

kuamua mambo yaliyo madogo
sana?[a] **3** Je, hamjui kwamba
tutawahukumu malaika?[b] Kwa
nini, basi, isiwe mambo ya mai-
sha haya? **4** Basi, ikiwa ninyi
mna mambo ya maisha haya
ya kuamuliwa,[c] je, mnawawe-
ka kuwa waamuzi wale watu
wanaodharauliwa na kutani-
ko?[d] **5** Ninasema ili kuwatia
ninyi aibu.[e] Je, ni kweli kwamba
hakuna hata mtu mmoja mwe-
nye hekima[f] kati yenu atakaye-
weza kuhukumu kati ya ndugu
zake, **6** bali ndugu anaenda
mahakamani pamoja na ndugu,
na tena mbele ya wasio waa-
mini?[g]

7 Basi, kwa kweli, inamaani-
sha kushindwa kwenu kabisa
kwamba mnakuwa na mashta-
ka ya kisheria[h] mtu na mwenza-
ke. Kwa nini msiache mkosewe[i]
badala ya hivyo? Kwa nini msia-
che mpunjwe[j] badala ya hivyo?
8 Kinyume cha hilo, mnawako-
sea na kuwapunja, tena ndugu
zenu.[k]

9 Kwani! Je, hamjui kwamba
watu wasio waadilifu hawatau-
rithi ufalme wa Mungu?[l] Msipo-
toshwe. Wala waasherati,[m] wala
waabudu-sanamu,[n] wala wazi-
nzi,[o] wala wanaume wanao-
wekwa kwa ajili ya makusu-
di yasiyo ya asili,[p] wala wa-
naume wanaolala na wanau-
me,[q] **10** wala wezi, wala watu
wenye pupa,[r] wala walevi,[s] wala
watukanaji, wala wanyang'a-
nyi hawataurithi ufalme wa
Mungu.[t] **11** Na bado wengi-
ne wenu mlikuwa hivyo.[u] Laki-
ni mmeoshwa mkawa safi,[v] la-
kini mmetakaswa,[w] lakini mme-
tangazwa kuwa waadilifu[x] ka-
tika jina la Bwana wetu Yesu
Kristo[y] na kwa roho ya Mungu
wetu.[z]

SURA 6

a 1Ko 4:3
b Ro 16:20
c Mt 18:17
d Met 29:27
e 1Ko 15:34
f Kum 1:13
1Ti 3:2
g 2Ko 6:15
h 2Nya 19:8
Lu 12:13
i Met 20:22
Mt 5:39
Ro 12:17
1Th 5:15
1Pe 3:9
j Zb 146:7
k 1Th 4:6
l Efe 5:5
Ufu 22:15
m Ufu 21:8
n Kol 3:5
o Ebr 13:4
p Ro 1:27
q 1Ti 1:10
r 1Ko 5:11
s Kum 21:20
Met 23:20
1Pe 4:3
t Ebr 12:14
1Pe 4:18
u Kol 3:7
Tit 3:3
v Yoh 13:10
Mdo 22:16
Ebr 10:22
w Efe 5:26
2Th 2:13
x Ro 5:18
y 1Yo 2:12
z Ro 8:33

Safu ya 2

a 1Ko 10:23
b Ro 6:14
c Ro 6:16
d Tit 1:12
e Ro 14:17
f 1Th 4:3
g Kol 1:18
1Th 5:23
h Mdo 2:24
Ro 6:4
Efe 1:20
i Ro 6:5
Ro 8:11
2Ko 4:14
j Efe 1:19
k 1Ko 12:18
1Ko 12:27
Efe 5:30
l Ro 12:5
Efe 4:15
m Yak 4:4
n Mwa 2:24
Mt 19:5
Efe 5:31
o Efe 4:3
Efe 4:4
p Yoh 17:21
q Mwa 39:12
1Th 4:3
r Ro 1:24
Ro 1:27
Ro 6:12
s 1Ko 3:16
2Ko 6:16
t 1Th 4:8
u Ro 14:8
v 1Ko 7:23
Ebr 9:12
1Pe 1:18
w Mt 5:16

12 Mambo yote ni halali kwa-
ngu; lakini si mambo yote ye-
nye faida.[a] Mambo yote ni hala-
li[b] kwangu; lakini mimi sitaru-
husu kitu chochote kinitawale.[c]
13 Vyakula kwa ajili ya tumbo,
na tumbo kwa ajili ya vyaku-
la;[d] lakini Mungu atafanya hilo
na pia hivyo viwe si kitu.[e] Basi
mwili si kwa ajili ya uashera-
ti, bali kwa ajili ya Bwana;[f]
na Bwana ni kwa ajili ya mwi-
li.[g] **14** Lakini Mungu alimfu-
fua Bwana[h] na pia atatufufua
sisi kutoka kwenye kifo[i] kupitia
nguvu zake.[j]

15 Je, hamjui kwamba mii-
li yenu ni viungo[k] vya Kristo?[l]
Basi, je, nitavichukua viungo
vya Kristo na kuvifanya kuwa
viungo vya kahaba?[m] Hilo lisite-
ndeke kamwe! **16** Kwani! Je,
hamjui kwamba yeye ambaye
ameungana na kahaba ni mwili
mmoja naye? Kwa maana, "Hao
wawili," yeye asema, "watuku-
wa mwili mmoja."[n] **17** Laki-
ni yeye ambaye ameungana na
Bwana ni roho[o] moja[p] naye.
18 Ukimbieni uasherati.[q] Kila
dhambi nyingine ambayo mtu
huenda akafanya iko nje ya
mwili wake, lakini yeye aliye
na mazoea ya kufanya uashe-
rati anautendea dhambi mwi-
li[r] wake mwenyewe. **19** Kwa-
ni! Je, hamjui kwamba mwili
wenu ni hekalu[s] la roho takatifu
ndani yenu,[t] mliyo nayo kutoka
kwa Mungu? Pia, ninyi si mali
yenu wenyewe,[u] **20** kwa maa-
na mlinunuliwa kwa bei.[v] Kwa
vyovyote, mtukuzeni[w] Mungu
katika mwili[x] wenu.

7 Basi kuhusu mambo amba-
yo mliandika habari zake,
ni vema mwanamume asimgu-

x Ro 12:1; 1Ko 12:27; Efe 4:12.

se[a] mwanamke; **2** lakini, kwa
sababu ya kuenea kwa uasherati,[b] kila mwanamume na awe
na mke[c] wake mwenyewe na kila
mwanamke awe na mume wake
mwenyewe. **3** Mume na ampe
mke wake haki[d] yake; lakini mke pia na amfanyie vivyo hivyo mume wake.[e] **4** Mke hana
mamlaka juu ya mwili wake
mwenyewe, bali mume wake
anayo;[f] vivyo hivyo, pia, mume
hana mamlaka juu ya mwili
wake mwenyewe, bali mke wake
anayo.[g] **5** Msiwe mkinyimana
haki hiyo,[h] ila kwa makubaliano kwa wakati uliowekwa,[i] ili
mtenge wakati kwa ajili ya sala
na mje pamoja tena, ili Shetani
asiendelee kuwajaribu[j] kwa sababu ya ninyi kukosa kujizuia.[k]
6 Hata hivyo, nasema hilo kwa
njia ya kutoa ruhusa,[l] si kwa njia
ya amri.[m] **7** Lakini ningalipenda watu wote wawe kama mimi
mwenyewe nilivyo.[n] Hata hivyo,
kila mmoja ana zawadi[o] yake
mwenyewe kutoka kwa Mungu,
mmoja kwa njia hii, mwingine
kwa njia ile.

8 Sasa nawaambia waseja[p]
na wajane, ni vema kwao wabaki kama mimi nilivyo.[q] **9** Lakini ikiwa hawawezi kujizuia,[r]
acheni wafunge ndoa,[s] kwa maana ni bora kufunga ndoa kuliko kuwaka tamaa.[t]

10 Kwa watu waliofunga
ndoa natoa maagizo, lakini si
mimi bali ni Bwana,[u] kwamba
mke hapaswi kuondoka kwa
mume wake;[v] **11** lakini kwa
kweli akiondoka, na akae mseja kama sivyo apatane tena na
mume wake; na mume hapaswi
kumwacha mke wake.

12 Lakini kwa wale wengine nawaaambia, ndiyo, mimi,
si Bwana:[w] Ikiwa ndugu ye-

SURA 7

a Mwa 20:6
Kum 22:28
Met 6:29
b Yer 5:7
1Th 4:3
c Mwa 2:24
Met 5:19
Ebr 13:4
d Kut 21:10
1Ko 7:5
e Ho 3:3
1Pe 3:7
f Efe 5:24
g Efe 5:21
h Mwa 4:1
1Sa 1:19
Mt 1:25
Ebr 13:4
i Kut 19:15
j 2Ko 2:11
1Th 3:5
k 1Ko 9:25
l Mt 19:8
m 1Ko 7:25
2Ko 8:8
n 1Ko 9:5
o Mt 19:11
p 1Ko 7:27
q 1Ko 9:5
r 1Th 4:4
1Ti 5:11
s 1Ti 5:14
t 1Th 4:5
u Mt 5:32
v Yer 3:20
Mt 19:6
Mk 10:11
Lu 16:18
w 1Ko 7:25

Safu ya 2

a Efe 6:1
b Ro 11:16
c Mal 2:15
d Ebr 12:14
e 1Pe 3:1
f Yak 5:20
g Zb 143:10
Isa 46:11
1Ko 12:18
h 1Ko 7:7
i 1Ko 9:14
j Mdo 21:20
k Mdo 10:45
Ga 5:2
l Mdo 15:1
Mdo 15:24
m Ro 2:25
n Ga 6:15
Kol 3:11
o Mhu 12:13
Yer 7:23
Ga 5:6
1Yo 5:3
p Efe 4:1
q 1Ko 7:17
r Ga 3:28

yote ana mke asiyeamini, na
bado mke huyo anakubali kukaa pamoja naye, basi asimwache; **13** na mwanamke aliye
na mume asiyeamini, na bado
mume huyo anakubali kukaa
pamoja naye, basi asimwache
mume wake. **14** Kwa maana
mume asiyeamini hutakaswa
kuhusiana na mke wake, na
mke asiyeamini hutakaswa kuhusiana na huyo ndugu; kama
sivyo, watoto wenu kwa kweli
hawangekuwa safi,[a] lakini sasa
wao ni watakatifu.[b] **15** Lakini yule asiyeamini akiondoka,
acha aondoke;[c] ndugu au dada
hayumo katika utumwa chini
ya hali za namna hiyo, lakini
Mungu amewaita ninyi kwenye
amani.[d] **16** Kwa maana, wewe
mke, unajuaje kama utamwokoa mume wako?[e] Au, wewe
mume, unajuaje kama utamwokoa mke wako?[f]

17 Isipokuwa, kama Yehova
alivyompa kila mmoja fungu,[g]
kila mmoja na ajiendeshe kama
Mungu alivyomwita.[h] Na ndivyo ninavyoagiza[i] katika makutaniko yote. **18** Je, mtu yeyote aliitwa akiwa ametahiriwa?[j]
Acheni asiwe asiyetahiriwa. Je,
mtu yeyote ameitwa akiwa katika kutotahiriwa?[k] Acheni asitahiriwe.[l] **19** Kutahiriwa[m] hakumaanishi kitu, na kutotahiriwa[n] hakumaanishi kitu, lakini kushika amri za Mungu kuna
maana.[o] **20** Katika hali yoyote ile ambayo kila mmoja aliitwa,[p] acheni abaki katika hiyo.[q]
21 Je, uliitwa ukiwa mtumwa?
Usiache hilo likutie wasiwasi;[r]
lakini ikiwa unaweza pia kuwa
huru, afadhali utwae nafasi
hiyo. **22** Kwa maana yeyote
katika Bwana aliyeitwa akiwa
mtumwa ni mtu aliyewekwa

huru wa Bwana;[a] vivyo hivyo
yeye aliyeitwa akiwa mtu ali-
ye huru[b] ni mtumwa[c] wa Kristo.
23 Mlinunuliwa kwa bei;[d] ache-
ni kuwa watumwa[e] wa wanada-
mu. **24** Katika hali[f] yoyote ile
ambayo kila mmoja aliitwa, aki-
na ndugu, acheni abaki katika
hali hiyo akishirikiana na Mu-
ngu.

25 Sasa kuhusu mabikira
sina amri kutoka kwa Bwana,
lakini natoa maoni[g] yangu niki-
wa mtu aliyeonyeshwa rehe-
ma na Bwana[h] kuwa mwami-
nifu.[i] **26** Kwa hiyo naona hili
kuwa ni jema kwa sababu ya
uhitaji uliopo pamoja nasi, kwa-
mba ni vema kwa mtu kue-
ndelea kama alivyo.[j] **27** Je,
umefungwa kwa mke?[k] Uache
kutafuta kufunguliwa.[l] Je, ume-
funguliwa kutoka kwa mke?
Uache kutafuta mke. **28** La-
kini hata kama ukifunga ndoa,
hutakuwa ukifanya dhambi.[m]
Na kama bikira akifunga ndoa,
mtu huyo hatakuwa akifanya
dhambi. Hata hivyo, wale wana-
ofanya hivyo watakuwa na dhi-
ki katika mwili wao.[n] Lakini
mimi ninawaepusha ninyi.

29 Zaidi ya hayo, nasema
hili, akina ndugu, wakati ulio-
baki umepungua.[o] Tangu sasa
wale walio na wake na wawe
kana kwamba hawana,[p] **30** na
pia wale wanaolia wawe kama
wale wasiolia, na wale wanao-
shangilia wawe kama wale wa-
siosheshangilia, na wale wanaonu-
nua wawe kama wale wasio na
kitu, **31** na wale wanaoutu-
mia ulimwengu[q] wawe kama
wale wasioutumia kwa uka-
mili; kwa maana tamasha ya
ulimwengu huu inabadilika.[r]
32 Kwa kweli, nataka ninyi
msiwe na mahangaiko.[s] Mwa-

SURA 7

a Yoh 8:36
Flm 16
b Efe 6:8
c 1Pe 2:16
d 1Ko 6:20
Ebr 9:12
1Pe 1:18
e Ga 4:9
Ga 5:1
f 1Ko 7:26
g 1Ko 7:12
h 1Ti 1:16
i 1Ti 1:12
j 1Ko 7:17
k Mt 19:6
l Mal 2:16
Efe 5:33
m Ebr 13:4
n Mwa 3:16
o Mt 24:33
Ro 13:11
1Pe 4:7
p Lu 14:26
q 1Yo 2:16
r 2Ti 3:13
s Lu 10:41

Safu ya 2

a Lu 14:20
1Ti 5:8
b 1Ko 7:4
c Lu 10:42
1Ti 5:5
d Met 31:12
e 1Ko 6:12
f Lu 10:40
g Mt 19:12
h 1Ko 7:28
i Mt 19:11
j Ebr 13:4
k 1Ko 7:32
l Ro 7:2

namume ambaye hajaoa huhan-
gaikia mambo ya Bwana, jinsi
anavyoweza kupata kibali cha
Bwana. **33** Lakini mwanamu-
me aliyeoa huhangaikia[a] ma-
mbo ya ulimwengu, jinsi ana-
vyoweza kupata kibali cha mke
wake,[b] **34** naye amegawanyi-
ka. Zaidi ya hayo, mwanamke
mseja, na bikira, huhangaikia
mambo ya Bwana,[c] ili awe mta-
katifu katika mwili wake na pia
katika roho yake. Hata hivyo,
mwanamke aliyeolewa huha-
ngaikia mambo ya ulimwengu,
jinsi anavyoweza kupata kiba-
li cha mume wake.[d] **35** Laki-
ni nasema jambo hili kwa faida
yenu ya kibinafsi, si ili niwa-
tegee mtego, bali ili niwasuku-
me ninyi kwenye lile linalofaa[e]
na lile linalomaanisha kumhu-
dumia Bwana daima bila kuke-
ngeushwa fikira.[f]

36 Lakini kama yeyote aki-
ona kwamba anajiendesha isi-
yofaa kuelekea ubikira[g] wake,
ikiwa huo umepita upeo wa uja-
na, na hivyo ndivyo inavyopa-
swa kutendeka, acheni afanye
lile analotaka; hafanyi dhambi.
Acheni afunge ndoa.[h] **37** La-
kini ikiwa yeyote ametulia kati-
ka moyo wake, akiwa hana uhi-
taji wowote, lakini ana mamla-
ka juu ya nia yake mwenyewe
naye amefanya uamuzi huu ka-
tika moyo wake mwenyewe, ku-
tunza ubikira wake mwenyewe,
yeye atafanya vema.[i] **38** Kwa
hiyo yeye pia anayeufungisha
ndoa ubikira wake anafanya
vema,[j] lakini yeye asiyeufungi-
sha ndoa atafanya vema zaidi.[k]

39 Mke amefungwa wakati
wote ambao mume wake yuko
hai.[l] Lakini mume wake akilala
usingizi katika kifo, yeye yuko
huru kuolewa na yeyote ana-

yemtaka, katika Bwana tu.[a]
40 Lakini mwanamke huyo ni
mwenye furaha zaidi akibaki
kama alivyo,[b] kwa maoni yangu.
Hakika nafikiri mimi pia nina
roho ya Mungu.[c]

8 Basi kuhusu vyakula vina-
vyotolewa kwa sanamu:[d]
tunajua sisi sote tuna ujuzi.[e]
Ujuzi huleta majivuno, laki-
ni upendo hujenga.[f] **2** Yeyo-
te akifikiri amejipatia ujuzi juu
ya kitu fulani,[g] bado hajaki-
jua kama vile anavyopaswa ku-
kijua.[h] **3** Lakini ikiwa yeyote
anampenda Mungu,[i] huyo ana-
julikana naye.[j]
4 Sasa kuhusu kula[k] vya-
kula vinavyotolewa kwa sa-
namu, tunajua kwamba sana-
mu si kitu[l] katika ulimwengu,
na kwamba hakuna Mungu isi-
pokuwa mmoja.[m] **5** Kwa maa-
na hata ingawa kuna wale wana-
oitwa "miungu,"[n] iwe wako mbi-
nguni[o] au duniani,[p] kama vile
kulivyo na "miungu" mingi
na "mabwana" wengi,[q] **6** kwa
kweli kwetu sisi kuna Mungu
mmoja[r] aliye Baba,[s] ambaye
vitu vyote vimetoka kwake, na
sisi kwa ajili yake;[t] na kuna
Bwana[u] mmoja, Yesu Kristo,[v]
ambaye vitu vyote vimepitia
kwake,[w] na sisi kupitia yeye.
7 Hata hivyo, si watu wote
walio na ujuzi huu;[x] bali we-
ngine, wakiwa wameizoea sa-
namu mpaka sasa, hula chaku-
la kama kitu kilichotolewa dha-
bihu kwa sanamu,[y] na dhamiri
yao, kwa kuwa ni dhaifu, ina-
tiwa unajisi.[z] **8** Lakini chaku-
la hakitatupendekeza kwa Mu-
ngu;[a] tukikosa kula, hatupu-
ngukiwi, na, tukila, hatupati
sifa kwetu wenyewe.[b] **9** Laki-
ni endeleeni kuangalia kwamba
hii mamlaka yenu isije kuwa
kwa njia fulani kikwazo kwa
wale walio dhaifu.[a] **10** Kwa
maana yeyote akikuona wewe,
uliye na ujuzi, ukiwa umeketi
kwenye mlo katika hekalu la sa-
namu, je, dhamiri ya huyo ali-
ye dhaifu haitajengwa kufikia
hatua ya kula vyakula vilivyo-
tolewa kwa sanamu?[b] **11** Kwa
kweli, kwa ujuzi wako, mtu
ambaye ni dhaifu anaharibiwa,
ndugu yako ambaye Kristo ali-
kufa kwa ajili yake.[c] **12** Laki-
ni ninyi mnapotenda dhambi hi-
vyo juu ya ndugu zenu na ku-
iumiza dhamiri[d] yao iliyo dhai-
fu, mnamtendea dhambi Kristo.
13 Kwa hiyo, ikiwa chakula ki-
namkwaza ndugu yangu,[e] mimi
sitakula nyama tena kamwe,
ili nisije nikamkwaza[f] ndugu
yangu.

9 Je, mimi si huru?[g] Je, mimi
si mtume?[h] Je, mimi sija-
mwona Yesu Bwana wetu?[i] Je,
ninyi si kazi yangu katika Bwa-
na? **2** Ikiwa mimi si mtume
kwa wengine, hakika mimi ni
mtume kwenu, kwa maana ni-
nyi ndio muhuri unaothibitis-
ha[j] utume wangu kuhusiana na
Bwana.
3 Kwa wale wanaonichunguz-
za, najitetea hivi:[k] **4** Sisi tuna
mamlaka ya kula[l] na kunywa, si-
vyo? **5** Sisi tuna mamlaka ya
kumchukua pamoja nasi dada
akiwa mke,[m] hata kama vile mi-
tume wale wengine na ndugu za
Bwana[n] na Kefa,[o] sivyo? **6** Au
je, ni Barnaba[p] na mimi peke
yetu tusio na mamlaka ya kuji-
epusha kufanya kazi ya kimwi-
li?[q] **7** Ni nani ambaye hutumi-
ka akiwa askari kwa gharama
yake mwenyewe? Ni nani amba-
ye hupanda shamba la mizabi-
bu na asile matunda yake?[r] Au
ni nani ambaye huchunga kundi

SURA 7

a Mwa 24:3
Kum 7:3
Kum 7:4
Ne 13:25
2Ko 6:14
b 1Ko 7:26
c 1Th 4:8

SURA 8

d Mdo 15:20
e Ro 14:14
1Ko 8:10
f 1Ko 8:13
1Ko 13:5
Efe 3:19
g Ga 6:3
h 1Ti 6:4
i 1Yo 4:8
j Kut 33:12
Nah 1:7
k 1Ko 10:18
l Kum 32:21
2Fa 19:18
Isa 44:10
Yer 16:20
m Kum 6:4
Kum 32:39
Efe 4:6
n Zb 82:1
Yoh 10:35
o Zb 8:5
Ebr 2:7
p Zb 82:6
q Zb 136:3
r 1Ti 2:5
s Mal 2:10
Mt 23:9
t Mdo 17:28
Ro 11:36
u Efe 4:5
v Flp 2:11
w Yoh 1:3
Kol 1:16
x Ro 14:14
1Ko 10:27
y 1Ko 10:28
z Ro 14:23
a Ro 14:17
b Ebr 13:9

Safu ya 2

a Ro 14:13
Ro 14:20
b Ufu 2:14
c Mt 20:28
Ro 14:15
d 1Ko 10:29
e Ro 14:15
f Mt 18:6
Ro 14:21
2Ko 11:29

SURA 9

g Ga 5:1
h 2Ko 12:12
1Ti 2:7
i Mdo 9:5
1Ko 15:8
j 2Ko 3:2
k 1Ko 4:3
l Lu 10:8
m Mt 19:11
n Mt 13:55
Ga 1:19
o Mt 8:14
Yoh 1:42
p Mdo 13:2
q Mdo 18:3
2Th 3:8
r Kum 20:6
Met 27:18

na asinywe sehemu ya maziwa
ya kundi?[a]
8 Je, ninasema mambo haya
kwa viwango vya kibinadamu?[b]
Au je, Sheria[c] haisemi mambo
hayo pia? **9** Kwa maana kati-
ka sheria ya Musa imeandikwa:
"Hupaswi kumfunga kinywa
ng'ombe-dume anapopura nafa-
ka."[d] Je, ni ng'ombe ambao Mu-
ngu anajali? **10** Au, je, yeye
hasemi hilo kwa ajili yetu tu?
Kwa kweli hilo liliandikwa kwa
ajili yetu,[e] kwa sababu mtu ana-
yelima anapaswa kulima aki-
wa na tumaini na mtu anayepu-
ra anapaswa kupura akiwa na
tumaini la kula.[f]
11 Ikiwa tumepanda vitu
vya kiroho[g] kwenu, je, ni jambo
kubwa tukivuna kutoka kwenu
vitu vilivyo kwa ajili ya mwili?[h]
12 Ikiwa watu wengine hushi-
riki mamlaka hii juu yenu,[i] je,
si hivyo hata zaidi kwetu? Hata
hivyo, sisi hatujatumia mamla-
ka hii,[j] bali tunavumilia mambo
yote, ili tusiweke kizuizi cho-
chote kwa habari njema[k] juu
ya Kristo. **13** Je, hamjui kwa-
mba watu wanaofanya kazi ta-
katifu hula[l] vitu vya hekalu,
na wale wanaohudumu[m] daima
kwenye madhabahu hupa-
ta fungu lao wenyewe pamoja
na madhabahu? **14** Vivyo hi-
vyo, pia, Bwana aliagiza[n] kuwa
wale wanaotangaza habari nje-
ma waishi kwa njia ya habari
njema.[o]
15 Lakini mimi sijatumia
hata mmoja wa mipango hiyo.[p]
Kwa kweli, sijaandika mambo
haya ili iwe hivyo kuhusiana
na mimi, kwa maana ingeku-
wa vizuri zaidi kwangu nife
kuliko—hakuna mtu atakaye-
fanya sababu yangu ya kujisifu[q]
iwe bure! **16** Ikiwa, sasa, nina-

SURA 9

a Kum 32:14
1Pe 5:2
b Ro 3:5
c Zb 19:7
d Kum 25:4
1Ti 5:18
e Ro 15:4
1Ko 10:11
f 2Ti 2:6
g 1Ko 2:13
Ga 1:11
h Ro 15:27
Ga 6:6
Flp 4:17
i Mt 17:25
Lu 20:25
j Mdo 20:34
k 2Ko 6:3
2Ko 11:7
l Law 6:16
Hes 18:31
Kum 18:1
m 1Ko 7:35
n Mt 10:10
Lu 10:7
o Ro 15:27
Ga 6:6
1Th 2:9
Ebr 13:16
p Mdo 18:3
Mdo 20:34
1Ko 4:12
2Th 3:8
q 2Ko 11:10

Safu ya 2

a Ufu 22:17
b Yer 20:9
Lu 17:10
c Eze 3:18
d 1Pe 5:2
e 1Ko 3:14
f Ga 2:7
Efe 3:2
Kol 1:25
g 2Ko 11:7
h Ga 5:13
i 1Pe 3:1
j Mdo 16:3
Mdo 18:18
k Mdo 21:24
Mdo 21:26
l Ro 6:14
m Ro 2:12
n Ga 2:3
o Yoh 13:34
Ga 6:2
p 1Ko 7:22
q Ro 14:1
Ro 15:1
2Ko 11:29
r Ga 3:28
s Mdo 19:26
1Th 2:8
t Ga 5:7
u Flp 3:14
Kol 2:18
v Ga 2:2
Flp 2:16
w Mt 10:22
Mt 24:13
2Ti 4:8

tangaza habari njema,[a] hiyo si
sababu ya mimi kujisifu, kwa
maana nimewekewa sharti.[b]
Kwa kweli, ole[c] wangu mimi
ikiwa sitangazi habari njema!
17 Kama nikifanya hilo kwa
kupenda,[d] nina thawabu;[e] laki-
ni kama nikifanya hilo kinyume
cha kupenda kwangu, vyovyote
vile nina usimamizi-nyumba[f] ni-
liokabidhiwa. **18** Basi, thawa-
bu yangu ni nini? Kwamba nina-
potangaza habari njema niitoe
habari njema bila gharama,[g] ku-
sudi nisitumie vibaya mamlaka
yangu katika habari njema.
19 Kwa maana, ingawa niko
huru kutoka kwa watu wote, ni-
mejifanya kuwa mtumwa[h] kwa
wote, ili niwapate[i] watu walio
wengi zaidi. **20** Na kwa hiyo
kwa Wayahudi[j] nilikuwa kama
Myahudi, ili niwapate Wayahu-
di; kwa wale walio chini ya she-
ria nilikuwa kama aliye chini ya
sheria,[k] ingawa mimi mwenye-
we siko chini ya sheria,[l] ili niwa-
pate wale walio chini ya sheria.
21 Kwa wale wasio na sheria[m]
nilikuwa kama asiye na sheria,[n]
ijapokuwa mimi siko bila sheria
kwa Mungu bali niko chini ya
sheria[o] kwa Kristo,[p] ili niwapate
wale wasio na sheria. **22** Kwa
walio dhaifu nilikuwa dhaifu, ili
niwapate walio dhaifu.[q] Nime-
kuwa mambo yote kwa watu wa
namna zote,[r] ili kwa vyovyote
niwaokoe wengine. **23** Lakini
ninafanya mambo yote kwa aji-
li ya habari njema, ili niishiriki[s]
hiyo pamoja na wengine.
24 Je, hamjui kwamba waki-
mbiaji[t] katika mbio wote huki-
mbia, lakini ni mmoja tu ana-
yepokea tuzo?[u] Kimbieni[v] kwa
namna ya kwamba mweze ku-
pata tuzo.[w] **25** Zaidi ya hayo,
kila mtu anayeshiriki katika

shindano hujizuia[a] katika mambo yote. Basi wao, bila shaka, hushindana ili wapate taji[b] linaloharibika, lakini sisi ili tupate taji lisiloharibika.[c] **26** Kwa hiyo, jinsi ninavyokimbia[d] si bila uhakika; jinsi ninavyoelekeza ngumi zangu ni ili nisiwe nikipiga hewa;[e] **27** lakini naupigapiga mwili[f] wangu na kuuongoza kama mtumwa, ili, baada ya mimi kuwahubiria wengine, mimi mwenyewe nisikataliwe[g] kwa njia fulani.

10 Basi sitaki mkose kujua, akina ndugu, kwamba mababu zetu walikuwa wote chini ya wingu[h] na wote walipita katika bahari[i] **2** na wote walibatizwa katika Musa[j] kupitia wingu na bahari; **3** na wote walikula chakula kilekile cha kiroho[k] **4** na wote walikunywa maji[l] yaleyale ya kiroho. Kwa maana walikuwa wakinywa kutokana na mwamba[m] wa kiroho uliowafuata, na mwamba[n] huo ulimaanisha Kristo.[o] **5** Hata hivyo, Mungu hakuonyesha kibali[p] chake juu ya walio wengi kati yao, kwa maana waliangamizwa[q] nyikani.

6 Basi mambo hayo yalikuwa vielelezo kwetu sisi, ili tusiwe watu wanaotamani mambo mabaya,[r] kama wao walivyoyatamani. **7** Wala tusiwe waabudu-sanamu, kama baadhi yao walivyofanya;[s] kama ilivyoandikwa: "Watu wakaketi ili wale na kunywa, nao wakasimama wapate kujifurahisha."[t] **8** Wala tusifanye uasherati, kama baadhi yao walivyofanya uasherati,[u] na kuanguka, 23,000 kati yao katika siku moja.[v] **9** Wala tusimjaribu Yehova,[w] kama baadhi yao walivyomjaribu,[x] na kuangamizwa na nyoka.[a] **10** Wala tusiwe wanung'unikaji, kama baadhi yao walivyonung'unika,[b] na kuangamizwa na mwangamizaji.[c] **11** Basi mambo hayo yaliendelea kuwapata kuwa vielelezo, nayo yaliandikwa ili kuwa onyo[d] kwetu sisi ambao tumefikiwa na miisho ya mifumo ya mambo.[e]

12 Kwa hiyo yeye anayefikiri kuwa amesimama na ajihadhari kwamba asianguke.[f] **13** Hakuna jaribu ambalo limewapata ninyi ila lile lililo kawaida kwa watu.[g] Lakini Mungu ni mwaminifu,[h] naye hatawaacha ninyi mjaribiwe kupita mnavyoweza kuhimili,[i] bali pamoja na hilo jaribu ataifanya pia njia ya kutokea[j] kusudi mweze kulivumilia.

14 Kwa hiyo, wapendwa wangu, ikimbieni[k] ibada ya sanamu.[l] **15** Nasema kana kwamba ni kwa watu wenye utambuzi;[m] hukumuni ninyi wenyewe lile ninalosema. **16** Kikombe[n] cha baraka ambacho tunabariki, je, hicho si kushiriki katika damu ya Kristo? Ule mkate ambao tunamega,[o] je, huo si kushiriki katika mwili wa Kristo?[p] **17** Kwa sababu kuna mkate mmoja, sisi, ingawa tuko wengi,[q] ni mwili mmoja,[r] kwa maana sisi sote tunakula huo mkate mmoja.[s]

18 Tazameni kile ambacho ni Israeli kwa njia ya kimwili:[t] Je, wale wanaokula dhabihu si washiriki pamoja na madhabahu?[u] **19** Basi, nisieme nini? Kwamba kile ambacho kimetolewa dhabihu kwa sanamu ni kitu, au kwamba sanamu ni kitu?[v] **20** Hapana; bali nasema kwamba vitu ambavyo mataifa huvitoa dhabihu wao

SURA 9
a 2Pe 1:6
b 2Ti 2:5
c Yak 1:12
d Ebr 12:1
e 1Ko 14:9
f Ro 8:13
Kol 3:5
g 2Ko 13:6

SURA 10
h Kut 13:21
i Kut 14:22
j Ebr 3:5
k Kut 16:15
l Kut 17:6
Zb 78:15
m Hes 20:11
n Mt 16:18
1Pe 2:4
o Yoh 4:10
Yoh 4:25
p Hes 14:16
Eze 20:15
Yud 5
q Hes 14:29
Ebr 3:17
r Hes 11:34
Zb 106:14
s Kut 32:4
t Kut 32:6
u Hes 25:1
2Pe 2:2
v Hes 25:9
w Kum 6:16
x Hes 21:5

Safu ya 2
a Hes 21:6
b Hes 14:2
c Kut 23:21
Hes 14:37
d Ro 15:4
e Ebr 9:26
1Pe 4:7
f Met 28:14
Lu 22:34
Ro 11:20
Ga 6:1
g 1Pe 5:9
h 1Th 5:24
2Th 3:3
i Lu 22:32
2Pe 2:9
j 1Sa 30:6
Isa 40:29
Mdo 27:44
Flp 4:13
k 2Ko 6:17
l Kum 4:25
Kol 3:5
1Yo 5:21
m 1Ko 14:20
n Mt 26:27
Lu 22:17
o Mt 26:26
Lu 22:19
p 1Ko 12:18
q Ro 12:5
1Ko 12:25
r Efe 4:4
s Yoh 6:33
Yoh 6:35
t Ro 9:8
u Law 7:15
v 1Ko 8:4

huvitoa dhabihu kwa roho waovu,[a] na si kwa Mungu; nami sitaki ninyi muwe washiriki pamoja
na roho waovu.[b] **21** Hamwezi kuwa mkinywa kikombe cha
Yehova[c] na kikombe cha roho waovu; hamwezi kuwa mkishiriki "meza ya Yehova"[d] na meza
ya roho waovu. **22** Au je, "tunamchochea Yehova kuwa na
wivu"?[e] Je, sisi tuna nguvu[f] zaidi kuliko yeye?

23 Mambo yote ni halali; lakini si mambo yote yaliyo na faida.[g] Mambo yote ni halali;[h] lakini si mambo yote yanayojenga.[i]
24 Kila mmoja na aendelee kutafuta, si faida yake mwenyewe,[j]
bali ile ya yule mtu mwingine.[k]

25 Endeleeni kula kila kitu kinachouzwa katika soko la nyama,[l] bila kuchunguza kwa sababu ya dhamiri yenu;[m] **26** kwa
maana "dunia na vyote vinavyoijaza[n] ni vya Yehova."[o] **27** Yeyote kati ya wasio waamini akiwaalika nanyi mtake kwenda,
kuleni kila kitu kinachowekwa mbele yenu,[p] bila kuchunguza
kwa sababu ya dhamiri yenu.[q]
28 Lakini yeyote akiwaambia ninyi: "Hiki ni kitu kilichotolewa katika dhabihu," msile kwa
sababu ya yule aliyefunua hilo na kwa sababu ya dhamiri.[r]
29 "Dhamiri," nasema, si yako mwenyewe, bali ile ya yule mtu
mwingine. Kwa maana kwa nini iwe kwamba uhuru wangu
unahukumiwa na dhamiri ya mtu mwingine?[s] **30** Ikiwa nakula nikiwa na shukrani, kwa
nini nitukanwe juu ya kile ninachotolea shukrani?[t]

31 Kwa hiyo, kama mnakula au mnakunywa au mnafanya jambo lingine lolote, fanyeni mambo yote kwa utukufu wa
Mungu.[u] **32** Epukeni kuwa vi-

SURA 10
a Kum 32:17; Zb 106:37
b Yud 6
c Zb 116:13
d Eze 41:22; Mal 1:12
e Kut 34:14; Kum 32:21
f Ayu 9:4
g 1Ko 6:12
h Ro 6:14
i Ro 14:19; Ro 15:2
j 1Ko 10:33; 1Ko 13:5; Flp 2:21
k Flp 2:4
l 1Ti 4:4
m Ro 14:22
n Zb 24:1
o Kut 19:5; Kum 10:14
p Lu 10:8
q 1Ko 8:7
r 1Ko 8:10
s Ro 14:16; 1Ko 8:12
t Ro 14:6; 1Ti 4:3
u Mt 5:16; Kol 3:17; 1Pe 4:11

Safu ya 2
a Ro 14:13; 1Ko 8:13; 2Ko 6:3
b 1Ko 9:22
c Ro 15:2; Flp 2:4
d 1Th 2:16

SURA 11
e Flp 3:17; 2Th 3:9
f 1Ko 4:17; 2Th 2:15; 2Th 3:6
g Ro 14:9; Efe 4:15; Kol 2:10
h Mwa 3:16; Efe 5:23; 1Pe 3:1
i 1Ko 15:27; 1Ko 15:28
j Efe 4:15
k Yoe 2:28; Mdo 21:9
l Efe 5:23
m Yer 7:29; 1Ko 11:15
n Kum 21:12
o Mwa 24:65
p Mwa 1:27; Yak 3:9
q Ro 3:23
r Mwa 2:23
s Mwa 2:22

kwazo[a] kwa Wayahudi na vilevile kwa Wagiriki na kwa kutaniko la Mungu, **33** kama vile
mimi ninavyowapendeza watu wote katika mambo yote,[b] bila
kutafuta faida yangu mwenyewe[c] bali ile ya walio wengi, ili wapate kuokolewa.[d]

11 Iweni waigaji wangu, kama vile mimi nilivyo mwigaji wa Kristo.[e]

2 Sasa nawasifu ninyi kwa sababu katika mambo yote
mnanikumbuka na mnayashika sana mapokeo[f] kama vile nilivyowapa ninyi. **3** Lakini nataka mjue kwamba kichwa cha
kila mwanamume ni Kristo;[g] nacho kichwa cha mwanamke ni
mwanamume;[h] nacho kichwa cha Kristo ni Mungu.[i] **4** Kila
mwanamume ambaye husali au kutoa unabii akiwa na kitu
juu ya kichwa chake hukiaibisha kichwa chake;[j] **5** lakini
kila mwanamke ambaye husali au kutoa unabii[k] kichwa cha
chake kikiwa hakijafunikwa hukiaibisha kichwa chake,[l] kwa maana ni kana kwamba yeye ni
mwanamke mwenye kichwa kilichonyolewa.[m] **6** Kwa maana
ikiwa mwanamke hajifuniki, na akatwe nywele pia; lakini ikiwa inafedhehesha kwa mwanamke kukatwa nywele au kunyolewa,[n] basi na afunikwe.[o]

7 Kwa maana mwanamume
hapaswi kufunika kichwa chake, kwa kuwa yeye ni mfano[p]
na utukufu wa Mungu;[q] lakini mwanamke ni utukufu wa
mwanamume.[r] **8** Kwa maana mwanamume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke alitoka katika mwanamume;[s] **9** na, zaidi ya hayo,
mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwa-

namke kwa ajili ya mwanamume.[a] **10** Ndiyo sababu mwanamke anapaswa kuwa na ishara
ya mamlaka juu ya kichwa chake[b] kwa sababu ya malaika.[c]

11 Tena, kuhusiana na Bwana mwanamke si bila mwanamume wala mwanamume si
bila mwanamke.[d] **12** Kwa maana kama vile mwanamke ametoka katika mwanamume,[e] vivyo hivyo pia mwanamume
kupitia silaha[a] za uadilifu upa-
nde wa mkono wa kuume na wa
kushoto, **8** kupitia utukufu
na aibu, kupitia habari ambazo
ni mbaya na habari ambazo ni
njema; kama wanaodanganya[b]
na bado ni wenye kusema kwe-
li, **9** kama wasiojulikana na
bado ni wenye kutambuliwa,[a]
kama wanaokufa na bado, taza-
ma! tunaishi,[b] kama wanaotiwa
nidhamu[c] na bado hatukabidhi-
wi kwenye kifo,[d] **10** kama wa-
lio na huzuni lakini wenye ku-
shangilia sikuzote, kama maski-
ni lakini wenye kuwatajirisha
wengi, kama wasio na kitu cho-
chote na bado wenye kuwa na
vitu vyote.[e]
11 Kinywa chetu kimefu-
nguliwa kwenu, enyi Wakori-
ntho, moyo[f] wetu umepanuka.
12 Ninyi hamjasongwa mka-
kosa nafasi ndani yetu,[g] laki-
ni mmesongwa mkakosa nafasi
katika upendo wenu mwororo.[h]
13 Kwa hiyo, yakiwa kama ma-
lipo—mimi nasema kana kwa-
mba ni kwa watoto[i]—ninyi, pia,
panukeni.
14 Msifungwe nira isivyo
sawa pamoja na wasio waami-
ni.[j] Kwa maana kuna ushirika
gani kati ya uadilifu na uasi-she-
ria?[k] Au nuru ina ushirika gani
na giza?[l] **15** Na zaidi, kuna
upatano gani kati ya Kristo na
Beliali?[m] Au mtu mwaminifu
ana fungu[n] gani na asiye mwa-
mini? **16** Na hekalu la Mungu
lina upatano gani na sanamu?[o]
Kwa maana sisi ni hekalu[p] la
Mungu aliye hai; kama Mungu
alivyosema: "Mimi nitakaa kati-
kati yao[q] na kutembea katikati
yao, nami nitakuwa Mungu wao,
nao watakuwa watu wangu."[r]
17 "'Kwa hiyo tokeni katikati
yao, na mjitenge,' asema Yehova,
'na mwache kugusa kitu kilicho
najisi'";[s] "'nami nitawakaribisha
ndani.'"[t] **18** "'Nami nitakuwa

SURA 5

a Isa 43:25
Ro 4:25
Ro 5:18
b Mdo 13:38
c Mt 28:19
d Flp 3:20
e Efe 6:20
f Mt 25:40
g 2Ko 2:14
h Ufu 22:17
i Yoh 8:46
Ebr 4:15
Ebr 7:26
j Law 16:21
Ebr 9:28
k Kum 21:23
Ro 1:17

SURA 6

l Mt 28:20
2Ko 5:20
m Ro 2:4
Ebr 12:15
n Isa 49:8
o Lu 4:19
p Yoh 9:4
Ebr 3:13
q Ro 14:13
r 1Ko 9:22
s 2Ko 4:2
t 2Ko 11:23
u Ufu 2:10
v 2Ko 11:27
w Efe 4:2
Kol 3:13
1Th 5:14
x Mik 6:8
Efe 4:32
y Ro 12:9
1Ti 1:5
z 1Ko 2:4
a 2Ko 10:4
Efe 6:11
b Mt 10:16

Safu ya 2

a Mdo 4:13
2Ko 4:10
b 2Ko 4:11
c Zb 118:18
Ebr 12:6
d Mdo 14:19
2Ko 4:9
e Flp 4:13
Ufu 2:9
f 2Ko 8:16
g 2Ko 12:15
h 1Pe 2:17
1Yo 4:20
i 1Ko 4:14
j Kut 23:32
Kum 7:3
1Fa 11:4
1Ko 7:39
k 1Ko 5:11
Yak 4:4
l Efe 5:8
m Mt 4:10
Ufu 12:7
n 1Ko 10:21
o 1Ko 10:14
p 1Ko 3:16
1Ko 6:19
q Kut 29:45
Law 26:11

r Law 26:12; Eze 37:27; Zek 8:8; s Isa 52:11; Yer 51:45; Ufu 18:4; t Eze 20:41; 2Ko 7:1.

baba kwenu,[a] nanyi mtakuwa
wana na mabinti kwangu,"[b] asema Yehova Mweza-Yote."[c]

7 Kwa hiyo, wapendwa, kwa
kuwa tuna ahadi hizi,[d] acheni tujisafishe[e] wenyewe kila
unajisi wa mwili na roho,[f] tukiukamilisha utakatifu katika
kumwogopa Mungu.[g]

2 Mtupe sisi nafasi.[h] Hatujamkosea yeyote, hatujamharibu yeyote, hatujamtumia yeyote kwa kujifaidi.[i] **3** Sisemi jambo hili ili niwahukumu ninyi. Kwa maana tayari nimesema kwamba ninyi mko ndani ya mioyo yetu ili kufa na kuishi pamoja nasi.[j] **4** Mimi nina uhuru mkubwa wa kusema kuwaelekea ninyi. Ninajisifu kwa njia kubwa kuhusiana nanyi.[k] Nimejawa na faraja,[l] ninafurika kwa shangwe katika taabu yetu yote.[m]

5 Kwa kweli, tulipofika Makedonia,[n] mwili wetu haukupata kitulizo,[o] bali tuliendelea kutaabishwa[p] katika kila namna —kulikuwa na mapigano nje, woga ndani. **6** Hata hivyo Mungu, ambaye huwafariji[q] wale walioshushwa chini, alitufariji kwa kuwapo kwa Tito; **7** lakini si kwa kuwapo kwake tu, bali pia kwa faraja ambayo alikuwa amefarijiwa juu yenu, kwa kuwa alituletea habari[r] tena juu ya tamaa yenu, kuomboleza kwenu, bidii yenu kwa ajili yangu; hivi kwamba nikashangilia zaidi tena.

8 Kwa hiyo hata kama niliwahuzunisha ninyi kwa barua yangu,[s] mimi sijuti juu ya jambo hilo. Hata kama hapo mwanzoni nilijuta juu ya jambo hilo, (naona kwamba barua hiyo iliwahuzunisha ninyi, ingawa ni kwa kitambo kidogo,) **9** sasa ninashangilia, si kwa sababu mlihuzunishwa tu, bali kwa sababu mlihuzunishwa kufikia kutubu;[a] kwa maana mlihuzunishwa kwa njia ya kimungu,[b] ili msipatwe na hasara katika jambo lolote kwa sababu yetu. **10** Kwa maana huzuni kwa njia ya kimungu hutokeza toba kuelekea wokovu na haipasi kujuta;[c] lakini huzuni ya ulimwengu hutokeza kifo.[d] **11** Kwa maana, tazama! jambo hili, kule kuhuzunishwa kwenu kwa njia ya kimungu,[e] kulitokeza katika ninyi hali ya bidii kubwa kama nini, ndiyo, kujiondolea wenyewe hatia, ndiyo, ghadhabu, ndiyo, woga, ndiyo, kutamani, ndiyo, bidii, ndiyo, kurekebisha kosa![f] Katika kila jambo mlijionyesha kuwa safi kiadili katika jambo hili. **12** Hakika, ijapokuwa niliwaandikia ninyi, nilifanya hivyo, si kwa ajili ya yeye aliyetenda kosa,[g] wala kwa ajili ya yeye aliyekosewa, bali ili bidii yenu kwa ajili yetu ifunuliwe katikati yenu machoni pa Mungu. **13** Ndiyo sababu sisi tumefarijiwa.

Hata hivyo, kwa kuongezea faraja yetu sisi tulishangilia kwa wingi hata zaidi kwa sababu ya shangwe ya Tito, kwa sababu roho[h] yake imeburudishwa na ninyi nyote. **14** Kwa maana ikiwa nimejisifu kwake kwa vyovyote juu yenu, sijapata aibu; lakini kama tulivyowaambia mambo yote katika kweli, ndivyo pia kujisifu[i] kwetu mbele ya Tito kumekuwa kweli. **15** Pia, upendo wake mwororo ni mwingi zaidi kuwaelekea ninyi, anapokumbuka utii[j] wenu nyote, ji-

SURA 6
a 2Sa 7:14
b Isa 43:6
Ho 1:10
Yoh 1:12
c Ufu 1:8

SURA 7
d 2Ko 6:16
2Pe 1:4
e 1Ti 3:9
1Yo 3:3
f Zek 13:2
Ro 12:1
1Ti 1:5
g 2Ko 1:12
Ufu 14:7
h Ro 12:10
2Ko 6:12
i Mdo 20:33
2Ko 12:17
j 2Ko 6:12
k 1Ko 1:4
2Ko 1:14
l 2Ko 1:4
m Flp 2:17
Flm 7
n Mdo 20:1
o 2Ko 2:13
p 2Ko 4:8
q 2Ko 1:3
r Met 25:25
s 2Ko 2:4
2Ko 10:10

Safu ya 2
a Yer 31:19
Mdo 26:20
b Mdo 8:22
c Zb 32:5
Mt 26:75
1Yo 1:9
d Mwa 4:13
Mt 27:5
Ebr 12:17
e Yer 3:25
Yer 50:4
Mdo 2:37
f Mt 3:8
Mdo 26:20
g 1Ko 5:5
1Ko 5:13
h Mwa 45:27
1Ko 16:18
i 2Ko 8:24
j 2Ko 2:9
Ebr 13:17

nsi mlivyompokea kwa kuogopa na kutetemeka. **16** Nashangilia kwamba katika kila njia niwe na uhodari mwingi kwa sababu yenu.[a]

8 Basi akina ndugu, tunawajulisha ninyi juu ya fadhili zisizostahiliwa za Mungu ambazo makutaniko ya Makedonia[b] yamepewa, **2** kwamba wakati wa jaribu kubwa chini ya mateso shangwe yao nyingi na umaskini mkubwa ulifanya utajiri wa ukarimu wao uwe mwingi.[c] **3** Kwa maana hilo lilikuwa kulingana na uwezo wao halisi,[d] ndiyo, mimi nashuhudia, kupita uwezo wao halisi, **4** nao kwa kupenda kwao wenyewe waliendelea kutuomba kwa kusihi sana wapate pendeleo la kutoa kwa fadhili na kushiriki katika huduma iliyokusudiwa watakatifu.[e] **5** Na si kama tulivyokuwa tumetumaini tu, bali kwanza walijitoa wenyewe kwa Bwana[f] na kwetu kupitia mapenzi ya Mungu. **6** Hilo lilituongoza tumtie moyo Tito[g] kwamba, kama vile yeye alivyokuwa ameanzisha hilo katikati yenu, vivyo hivyo pia akamilishe utoaji huu wenye fadhili kwa upande wenu. **7** Hata hivyo, kama vile mnavyozidi katika kila jambo,[h] katika imani na neno na ujuzi[i] na bidii yote na katika upendo huu wetu kwenu, ninyi pia mzidi katika utoaji huu wenye fadhili.

8 Sisemi kwa kuwaamuru ninyi,[j] bali ni kwa kufikiria bidii ya wengine na ili kuujaribu uhalisi wa upendo wenu. **9** Kwa maana mnazijua fadhili zisizostahiliwa za Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba ingawa alikuwa tajiri, alikuja kuwa maskini kwa ajili yenu,[a] ili muwe matajiri[b] kupitia umaskini wake.

10 Na katika jambo hili mimi natoa maoni:[c] kwa maana jambo hili ni lenye faida kwenu,[d] kwa kuwa tayari mwaka mmoja uliopita mlianzisha si kule kufanya tu bali pia kule kutaka kufanya;[e] **11** sasa, basi, malizeni pia kule kufanya hilo, ili, kama vile kulivyokuwa na utayari wa kutaka kufanya, vivyo hivyo pia kuwe kumaliza hilo kutokana na kile mlicho nacho. **12** Kwa maana ikiwa utayari upo kwanza, hukubalika zaidi kulingana na kile ambacho mtu anacho,[f] si kulingana na kile ambacho mtu hana. **13** Kwa maana sikusudii iwe rahisi kwa wengine,[g] lakini vigumu kwenu; **14** bali kwamba kupitia usawazisho wa ziada yenu sasa hivi ijazie upungufu wao, ili ziada yao pia ije kujazia upungufu wenu, ili usawazisho uwepo.[h] **15** Kama ilivyoandikwa: "Mtu aliyekuwa na vingi hakuwa na vingi mno, na mtu aliyekuwa na vichache hakuwa na vichache mno."[i]

16 Basi Mungu na apewe shukrani kwa kuiweka bidii ileile kwa ajili yenu katika moyo wa Tito,[j] **17** kwa sababu kwa kweli ameitikia hicho kitia-moyo, lakini, akiwa mwenye bidii sana, anaondoka ili kuja kwenu kwa kupenda kwake mwenyewe. **18** Lakini tunamtuma pamoja naye ndugu ambaye sifa yake kuhusiana na habari njema imeenea katika makutaniko yote. **19** Si hayo tu, bali pia makutaniko yalimweka yeye rasmi[k] kuwa mwandamani wetu safarini kuhusiana na zawadi hii ya fadhili ambayo tutaishughulikia kwa

SURA 7
a 2Th 3:4

SURA 8
b Ro 15:26
c Ro 12:8
d Mk 12:44
Mdo 11:29
2Ko 9:7
e Ro 15:25
1Ko 16:1
2Ko 9:1
f Ro 6:13
g 2Ko 12:18
h 2Ko 9:8
i 1Ko 1:5
j 1Ko 7:6

Safu ya 2
a Mt 8:20
Lu 9:58
Flp 2:7
b 2Ko 6:10
c 1Ko 7:25
d Mt 10:42
e 2Ko 9:2
1Ti 6:18
f Law 27:8
Kum 16:10
Kum 16:17
Met 3:27
Mk 12:43
Lu 21:3
g Mk 12:44
h 2Ko 9:12
i Kut 16:18
j 2Ko 12:18
k 1Ko 16:3

ajili ya utukufu[a] wa Bwana na
kwa uthibitisho wa akili yetu
iliyo tayari.[b] **20** Hivyo tuna-
epuka kupata lawama[c] kuto-
ka kwa mtu yeyote kuhusiana
na mchango[d] huu wa ukarimu
ambao sisi tutaushughulikia.
21 Kwa maana sisi "tunafanya
mpango wa unyoofu, si machoni
pa Yehova tu, bali pia machoni
pa wanadamu."[e]

22 Zaidi ya hayo, tunatuma
pamoja nao ndugu yetu amba-
ye mara nyingi tumemjaribu
tukaona katika mambo mengi
ana bidii, lakini sasa ni mwe-
nye bidii nyingi zaidi kwa sa-
babu ya uhakika wake mkubwa
katika ninyi. **23** Ingawa hi-
vyo, kama kuna swali lolote
kumhusu Tito, yeye ni mshiri-
ki pamoja nami na mfanyakazi
mwenzangu[f] kwa ajili ya faida
yenu; au kama ni kuhusu ndu-
gu zetu, wao ni mitume wa ma-
kutaniko na utukufu wa Kristo.
24 Kwa hiyo waonyesheni uthi-
bitisho wa upendo[g] wenu na wa
yale tuliyojisifu[h] juu yenu, mbe-
le ya makutaniko.

9 Basi kuhusu huduma[i] amba-
yo ni kwa ajili ya watakati-
fu, ni jambo la ziada mimi ku-
waandikia ninyi, **2** kwa maa-
na naujua utayari wenu
wa akili ambao najisifia kwa
Wamakedonia juu yenu, kwa-
mba Akaya imesimama tayari
kwa mwaka mmoja[j] sasa, na bi-
dii yenu imewachochea walio
wengi kati yao. **3** Lakini ni-
nawatuma akina ndugu, ili ku-
jisifu kwetu juu yenu kusiwe
kwa bure kwa habari hii, bali ili
muwe tayari kwelikweli,[k] kama
nilivyokuwa nikisema mngeku-
wa. **4** Kama sivyo, kwa njia
fulani, Wamakedonia wakija pa-
moja nami na kuwakuta mkiwa
hamko tayari, sisi—sisemi ninyi
—tutaona aibu katika huu uha-
kikisho wetu. **5** Kwa hiyo ni-
liona kuwa ni jambo la lazima
niwatie moyo akina ndugu wa-
tangulie kuja kwenu na kuita-
yarisha mapema zawadi yenu
ya ukarimu iliyoahidiwa hapo
mwanzoni,[a] ili kwamba hiyo iwe
tayari kama zawadi ya ukarimu
na si kama kitu kilichopatikana
kwa kunyang'anywa.[b]

6 Lakini kuhusu hili, yeye
anayepanda kwa uhaba[c] atavu-
na pia kwa uhaba; na yeye ana-
yepanda kwa wingi[d] atavuna
pia kwa wingi. **7** Kila mmo-
ja na afanye kama alivyoazimia
moyoni mwake, si kwa kutope-
nda[e] wala kwa kulazimishwa,
kwa maana Mungu humpenda
mtoaji mchangamfu.[f]

8 Zaidi ya hayo, Mungu ana-
weza kufanya fadhili zake zote
zisizostahiliwa ziwe nyingi ku-
waelekea ninyi, ili, ijapokuwa
sikuzote mna ujitoshelevu ka-
mili katika kila kitu, muwe na
vingi kwa ajili ya kila kazi nje-
ma.[g] **9** (Kama ilivyoandikwa:
"Amegawa kwa wingi, amewa-
pa maskini, uadilifu wake una-
endelea milele."[h] **10** Basi yeye
ambaye humgawia mpandaji wa
mbegu kwa wingi na mkate wa
kula[i] atawagawia na kuwazi-
dishia ninyi mbegu ili mpande
naye ataongeza mazao ya ua-
dilifu wenu.)[j] **11** Katika kila
kitu mnatajirishwa kwa ajili ya
kila namna ya ukarimu, ambao
hutokeza kupitia sisi wonye-
sho wa shukrani kwa Mungu;[k]
12 kwa sababu huduma ya utu-
mishi huu wa watu wote si ku-
gawa tu kwa wingi mahitaji ya
watakatifu[l] bali pia kuwa ma-
tajiri kwa maonyesho mengi ya

SURA 8
a 2Ko 4:15
b 2Ko 9:2
c 2Ko 6:3
d 1Ko 16:1
e Met 3:4
1Pe 2:12
f Flp 2:25
g 1Pe 1:22
1Pe 2:17
h 2Ko 7:14

SURA 9
i Ro 15:26
1Ko 16:1
2Ko 8:4
2Ko 9:12
j 2Ko 8:10
k 2Ko 8:6

Safu ya 2
a 2Ko 9:2
b Isa 32:8
c Met 11:24
Ga 6:7
d Met 19:17
Met 22:9
Mhu 11:1
Lu 6:38
e Kum 15:7
Kum 15:10
Met 22:8
f Kut 22:29
1Nya 29:17
Met 11:25
Mdo 20:35
Ro 12:8
Ebr 13:16
g Met 28:27
Mal 3:10
Efe 4:28
Flp 4:19
Tit 2:14
h Zb 112:9
i Kum 30:9
Isa 55:10
j Ho 10:12
k 2Ko 1:11
2Ko 4:15
l Ro 15:27
2Ko 8:14
Ga 6:6
Flp 4:18

shukrani kwa Mungu. **13** Kupitia uthibitisho ambao huduma hii hutoa, wao wanamtukuza Mungu kwa sababu mnajitiisha kwenye habari njema juu ya Kristo,[a] mnapotangaza waziwazi kuwa mko hivyo, na kwa sababu ninyi ni wakarimu katika mchango wenu kwao na kwa wote;[b] **14** nao kupitia dua kwa ajili yenu wanatamani kuwaona ninyi kwa sababu ya fadhili nyingi zaidi zisizostahiliwa[c] za Mungu juu yenu.

15 Mungu apewe shukrani kwa ajili ya zawadi yake ya bure isiyoelezeka.[d]

10 Basi mimi mwenyewe, Paulo, nawasihi ninyi kwa upole[e] na fadhili[f] za Kristo, ingawa kuonekana kwangu[g] katikati yenu ni kwa hali ya chini, lakini nisipokuwapo mimi ni jasiri kuwaelekea ninyi.[h] **2** Kwa kweli naomba kwamba, nitakapokuwapo, nisitumie ujasiri kwa uhakika ule ambao nategemea kuchukua hatua za kijasiri[i] juu ya wengine ambao wanatukadiria sisi kana kwamba tulitembea kulingana na tulivyo katika mwili. **3** Kwa maana ingawa tunatembea katika mwili,[j] hatupigi vita kulingana na tulivyo katika mwili.[k] **4** Kwa maana silaha za vita vyetu si za kimwili,[l] bali ni zenye nguvu kwa Mungu[m] kwa ajili ya kupindua ngome zenye nguvu. **5** Kwa maana sisi tunapindua mawazo na kila jambo lililo juu sana ambalo limeinuliwa kinyume cha ujuzi wa Mungu;[n] nasi tunaiteka kila fikira ili kuifanya imtii Kristo; **6** nasi tuko tayari kutoa adhabu kwa ajili ya kila kitu kisichotii,[o] mara tu utii wenu wenyewe utakapokuwa umeisha kutimizwa kikamilifu.[a]

7 Mnayatazama mambo kulingana na thamani yake ya jujuu.[b] Mtu yeyote akijitegemea mwenyewe kwamba ni wa Kristo, acheni yeye atie akilini tena jambo hili kwa ajili yake mwenyewe, kwamba, kama vile yeye alivyo wa Kristo, ndivyo na sisi pia.[c] **8** Kwa maana hata nikijisifu[d] mno kidogo juu ya mamlaka ambayo Bwana alitupa sisi ili tuwajenge wala si kuwabomoa ninyi,[e] mimi sitaaibishwa, **9** ili nisionekane kuwa nataka kuwatia ninyi hofu kwa barua zangu. **10** Kwa maana, wao husema: "Barua zake ni nzito na zenye nguvu nyingi, lakini kuwapo kwake mwenyewe kimwili ni dhaifu[f] na maneno yake ni yenye kudharaulika."[g] **11** Mtu wa namna hiyo na atie jambo hili akilini, kwamba kile tulicho katika neno letu kwa barua wakati hatupo, ndivyo tutakavyokuwa pia katika tendo tutakapokuwapo.[h] **12** Kwa maana sisi hatuthubutu kujiweka katika kikundi cha watu fulani au kujilinganisha na watu fulani ambao hujipendekeza wenyewe.[i] Hakika wao kwa kujipima wenyewe kwa wenyewe na kujilinganisha wenyewe kwa wenyewe, hawana uelewaji.[j]

13 Kwa upande wetu sisi tutajisifu, si nje ya mipaka yetu tuliyogawiwa,[k] bali kulingana na mpaka wa eneo ambalo Mungu alitugawia kwa kipimio, akilifanya lifike hadi kwenu.[l] **14** Kwa kweli sisi hatujinyooshi wenyewe kupita kiasi kana kwamba hatukuwafikia ninyi, kwa maana sisi tulikuwa wa kwanza kuja hadi kwenu katika kutangaza habari njema

SURA 9
a Ro 6:17
2Ko 7:15
b Mt 5:16
Ebr 13:16
Yak 1:27
1Yo 3:17
c Mdo 20:24
d Yoh 1:17
Ro 3:24
Ro 5:15
Efe 3:7

SURA 10
e Mt 11:29
f Mt 11:30
g 1Ko 2:3
h 2Ko 10:10
i 1Ko 4:21
2Ko 13:2
2Ko 13:10
j Ga 2:20
k Ro 8:13
Efe 6:12
l Mt 26:52
Ro 13:12
Efe 6:13
1Th 5:8
1Ti 1:18
2Ti 2:24
m Ro 8:14
2Ko 6:7
n 1Ko 1:19
1Ko 3:19
2Ti 2:25
o 1Ti 1:20
Ebr 12:10

Safu ya 2
a 2Ko 2:9
2Ko 7:15
b 2Ko 5:12
c 1Yo 4:6
d 2Ko 12:6
e 2Ko 13:10
Ebr 13:17
f 2Ko 10:1
Ga 4:13
g 2Ko 11:6
h 2Ko 12:20
2Ko 13:2
i 2Ko 3:1
2Ko 5:12
j Met 25:27
Met 26:12
Ga 6:3
Ga 6:4
k Ro 12:3
l Mdo 9:15
Ga 2:8

juu ya Kristo.[a] **15** Hapana,
hatujisifu katika kazi za jasho
za mtu mwingine nje ya mipaka
yetu tuliyogawiwa,[b] bali tuna-
tumainia kwamba, kadiri ima-
ni yenu inavyoongezwa,[c] ndi-
vyo sisi tutakavyofanywa wa-
kubwa katikati yenu kuhusiana
na eneo letu.[d] Ndipo tutakapo-
zidi hata zaidi, **16** kutangaza
habari njema kwenye nchi zilizo
ng'ambo yenu,[e] ili tusijisifu katika
eneo la mtu mwingine amba-
po mambo yamekwisha kutaya-
rishwa. **17** "Bali yeye anayeji-
sifu, na ajisifu katika Yehova."[f]
18 Kwa maana yule anayejipe-
ndekeza si ndiye ambaye huku-
baliwa,[g] bali ni yule mtu ambaye
Yehova[h] humpendekeza.[i]

11 Laiti mngenivumilia ka-
tika kukosa kidogo akili.[j]
Lakini, kwa kweli, ninyi mna-
nivumilia! **2** Kwa maana nina
wivu juu yenu kwa wivu wa ki-
mungu,[k] kwa maana mimi bina-
fsi niliwachumbia[l] ninyi mume[m]
mmoja ili niwatoe mkiwa bi-
kira safi kiadili[n] kwa Kristo.[o]
3 Lakini naogopa kwamba kwa
njia fulani, kama nyoka alivyo-
mshawishi Hawa[p] kwa ujanja
wake, huenda akili zenu zika-
haribiwa[q] kutoka kwenye unyo-
ofu wa moyo na usafi wa ki-
adili ambao unamfaa Kristo.[r]
4 Kwa maana, kama ilivyo, mtu
fulani akija na kuhubiri Yesu
mwingine tofauti na yule tuliye-
mhubiri,[s] au mkipokea roho nyi-
ngine tofauti na ile mliyopokea,[t]
au habari njema[u] nyingine tofa-
uti na ile mliyokubali, mnamvu-
milia kwa urahisi.[v] **5** Kwa ma-
ana naona kwamba hata katika
jambo moja sijawa mdogo[w] kwa
mitume wenu walio bora sana.[x]
6 Lakini hata kama sina usta-
di wa kusema,[y] hakika sivyo ni-
livyo katika ujuzi;[a] lakini katika
kila njia tuliwafunulia ninyi hilo
katika mambo yote.[b]
7 Au je, nilifanya dhambi kwa
kujinyenyekeza[c] ili ninyi mwi-
nuliwe, kwa sababu niliwatanga-
zia ninyi habari njema ya Mu-
ngu kwa furaha bila gharama?[d]
8 Niliyanyang'anya makutaniko mengine kwa kupokea vitu kutoka kwao ili niwahudumie ninyi;[e] **9** na bado nilipokuwa pamoja nanyi na nikapatwa na uhitaji, sikuwa mzigo kwa mtu hata mmoja,[f] kwa maana ndugu waliotoka Makedonia[g] walijazia kwa wingi upungufu wangu. Ndiyo, katika kila njia nilikaa mwenyewe bila kuwa mzigo kwenu nami nitakaa hivyo.[h] **10** Ni kweli[i] ya Kristo katika hali yangu kwamba huku kujisifu[j] kwangu hakutakomeshwa katika maeneo ya Akaya. **11** Kwa sababu gani? Je, ni kwa sababu siwapendi ninyi? Mungu anajua ninawapenda.[k]

12 Basi lile ninalofanya bado mimi nitalifanya,[l] ili nikatilie mbali kisingizio kutoka kwa wale wanaotaka kisingizio cha kupatikana kuwa sawa nasi katika cheo ambacho wanajisifia. **13** Kwa maana watu wa namna hiyo ni mitume wa uwongo, wafanyakazi wadanganyifu,[m] wakijigeuza wenyewe kuwa mitume wa Kristo.[n] **14** Na si ajabu, kwa maana Shetani mwenyewe huendelea kujigeuza mwenyewe kuwa malaika wa nuru.[o] **15** Kwa hiyo si jambo kubwa kama wahudumu[p] wake wakiendelea pia kujigeuza wenyewe kuwa wahudumu wa uadilifu. Lakini mwisho wao utakuwa kulingana na matendo yao.[q]

16 Nasema tena, Mtu yeyote asifikiri kwamba mimi sina

SURA 10

a 1Ko 3:10
1Ko 4:15
b Ro 15:20
c 2Th 1:3
d 1Ko 9:1
e Mdo 19:21
Ro 15:24
f Isa 65:16
Yer 9:24
1Ko 1:31
g Lu 18:14
h 1Sa 13:14
Met 29:26
i Ro 2:29
1Ko 4:5
2Ti 2:15

SURA 11

j 2Ko 5:13
k Flp 1:8
l Ufu 21:2
Ufu 21:9
Ufu 22:17
m Mk 2:19
n Efe 5:27
Kol 1:28
o Law 21:13
Efe 5:23
p Mwa 3:4
1Ti 2:14
q Yoh 8:44
1Ti 6:5
Ebr 13:9
2Pe 3:17
2Yo 8
r 1Ko 6:15
s Ga 1:7
t 1Yo 4:3
u Ga 1:8
v Flp 2:21
2Yo 10
w 1Ko 15:10
2Ko 11:23
x 2Ko 12:11
Ga 2:6
y Kut 4:10
2Ko 10:10

Safu ya 2

a 1Ko 2:13
b Efe 3:4
c 1Ko 2:3
2Ko 10:1
d Mdo 18:3
1Ko 9:18
e Flp 4:10
f 2Ko 12:13
g Flp 4:15
h 1Th 2:9
i Ro 9:1
j 1Ko 9:15
k 2Ko 6:11
2Ko 7:3
2Ko 12:15
l 1Ko 9:12
m Zb 101:7
Zb 119:118
Mdo 5:3
Efe 4:14
n Ro 16:18
2Ko 2:17
2Pe 2:1
o Ga 1:8
2Th 2:9
p Yoh 8:44
q Mt 16:27
Ro 2:6
Ga 5:10
Flp 3:19
2Ti 4:14

akili. Na bado, ikiwa kwa kweli
mnafikiri hivyo, mnikubali hata
ikiwa ni kana kwamba sina aki-
li, ili mimi vilevile nijisifu[a] kido-
go kwa kiasi fulani. **17** Lile ni-
nalosema nalisema, si kwa ku-
fuata kielelezo cha Bwana, bali
kama katika ukosefu wa akili,
katika uhakika huu wa kupita
kiasi ulio kawaida ya kujisifu.[b]
18 Kwa kuwa wengi wanajisifu
kulingana na mwili,[c] mimi pia
nitajisifu. **19** Kwa maana ni-
nyi mnawavumilia kwa furaha
watu wasio na akili, kwa kuwa
ninyi mna akili. **20** Kwa kwe-
li, mnamvumilia yeyote anaye-
wafanya ninyi kuwa watumwa,[d]
yeyote anayemeza kile mlicho
nacho, yeyote anayenyakua kile
mlicho nacho, yeyote anayejii-
nua mwenyewe juu yenu, yeyo-
te anayewapiga usoni.[e]
21 Nasema hili kwa aibu
yetu, kana kwamba cheo chetu
ni dhaifu.
Lakini mtu mwingine yeyo-
te akitenda kwa ujasiri katika
jambo fulani—mimi ninaongea
kwa kukosa akili[f]—mimi pia ni-
natenda kwa ujasiri katika ja-
mbo hilo. **22** Je, wao ni Wae-
brania? Mimi pia.[g] Je, wao ni
Waisraeli? Mimi pia. Je, wao ni
uzao wa Abrahamu? Mimi pia.[h]
23 Je, wao ni wahudumu wa
Kristo? Mimi najibu kama mwe-
nda-wazimu, mimi ni mhudumu
kwa njia yenye kutokeza hata
zaidi:[i] katika kazi za jasho kwa
wingi zaidi,[j] katika vifungo vya
gereza kwa wingi zaidi,[k] kati-
ka mapigo kwa kuzidi mno, kati-
ka kukaribia kufa mara nyingi.[l]
24 Kwa Wayahudi nilipokea
mara tano mapigo 40[m] kupu-
ngua moja, **25** mara tatu nili-
pigwa kwa fimbo,[n] mara moja

SURA 11
a 2Ko 10:8
b 1Ko 3:21
c Flp 3:4
d Ga 2:4
Ga 4:9
Ga 5:1
e Flp 3:19
f 2Ko 5:13
2Ko 12:11
g Mdo 22:3
h Ro 11:1
Flp 3:5
i 2Ko 11:5
j Ro 11:13
1Ko 15:10
k Mdo 16:24
l Mdo 9:16
2Ko 6:4
1Pe 2:21
m Kum 25:3
n Mdo 16:22

Safu ya 2
a Mdo 14:19
b Mdo 27:41
c Mdo 20:3
d Mdo 23:10
e Mdo 14:5
f Mdo 13:50
g Mdo 20:31
h 1Ko 4:11
i 2Ko 6:5
j 2Ko 2:4
Kol 2:1
k 1Ko 9:22
l 2Ko 12:5
m Mdo 9:24
n Mdo 9:25

SURA 12
o Mdo 2:17
Mdo 22:17

nilipigwa kwa mawe,[a] mara tatu
nilivunjikiwa na meli,[b] usiku
mmoja na mchana mmoja ni-
mekaa katika kilindi; **26** ka-
tika safari mara nyingi, kati-
ka hatari za kutokana na mito,
katika hatari za kutokana na
wanyang'anyi wa njia kuu,[c] ka-
tika hatari za kutokana na ja-
mii yangu[d] mwenyewe, kati-
ka hatari za kutokana na ma-
taifa,[e] katika hatari ndani ya
jiji,[f] katika hatari za nyikani,
katika hatari za baharini, katika
hatari za katikati ya ndugu wa
uwongo, **27** katika kazi ya ja-
sho na kutaabika, katika usiku
mwingi bila usingizi[g] mara nyi-
ngi, katika njaa na kiu,[h] katika
kuepukana na chakula[i] nyakati
nyingi, katika baridi na uchi.
28 Mbali na mambo hayo ya
aina ya nje, kuna kinachoni-
kaza ndani siku kwa siku, ha-
ngaiko kwa ajili ya makutaniko
yote.[j] **29** Ni nani aliye dhai-
fu,[k] nami si dhaifu? Ni nani ame-
kwazika, nami siwaki hasira?
30 Ikiwa ni lazima kujisifu,
mimi nitajisifu[l] juu ya mambo
yanayohusiana na udhaifu wa-
ngu. **31** Mungu na Baba ya
Bwana Yesu, naam, Yeye aliye
wa kusifiwa milele, anajua sise-
mi uwongo. **32** Katika Dama-
sko gavana aliye chini ya Are-
ta mfalme alikuwa akilinda jiji
la Wadamasko ili kunikamata,[m]
33 lakini nilishushwa kupitia
dirisha ukutani katika kapu[n]
kubwa nami nikaiponyoka mi-
kono yake.

12 Lazima nijisifu. Haina
faida; lakini nitaende-
lea katika maono[o] ya miujiza
na ufunuo wa Bwana. **2** Na-
mjua mtu mmoja katika muu-
ngano na Kristo ambaye, miaka

kumi na minne iliyopita—kama
ni katika mwili sijui, au ni
nje ya mwili sijui; Mungu ana-
jua—alinyakuliwa[a] akiwa hivyo
mpaka kwenye mbingu ya tatu.
3 Ndiyo, namjua mtu wa na-
mna hiyo—kama ni katika mwi-
li au bila mwili,[b] mimi sijui,
Mungu anajua— **4** kwamba
alinyakuliwa kuingia katika pa-
radiso[c] na kusikia maneno ya-
siyoweza kutamkwa ambayo si
halali mtu kuyasema. **5** Mimi
nitajisifu juu ya mtu wa na-
mna hiyo, lakini mimi sitajisifu
juu yangu mwenyewe, isipoku-
wa kwa habari ya udhaifu wa-
ngu.[d] **6** Kwa maana hata ni-
kitaka kujisifu,[e] sitakuwa mwe-
nye kukosa akili, kwa maana ni-
tasema kweli. Lakini naepuka,
ili yeyote asinihesabie sifa zaidi
ya kile anachoniona mimi kuwa
au anachosikia kutoka kwangu,
7 kwa sababu tu ya wingi wa
huo ufunuo.

Kwa hiyo, ili nisijione kuwa
nimeinuliwa mno,[f] nilipewa
mwiba katika mwili,[g] malai-
ka wa Shetani, aendelee ku-
nipiga kofi, ili nisijiinue kupi-
ta kiasi. **8** Kwa ajili ya hilo
mara tatu[h] nilimsihi Bwana
kwamba huo uniondoke; **9** na
bado kwa kweli akaniambia:
"Fadhili zangu zisizostahiliwa
zinakutosha[i] wewe; kwa maa-
na nguvu zangu zinakamili-
shwa katika udhaifu."[j] Kwa fu-
raha zaidi, basi, ni afadhali ni-
jisifu kwa habari ya udhaifu
wangu,[k] ili nguvu za Kristo zi-
baki juu yangu kama hema.
10 Kwa hiyo napendezwa na
udhaifu, na matusi, na hali za
uhitaji, na mateso na magumu,
kwa ajili ya Kristo. Kwa maana
ninapokuwa dhaifu, ndipo nina-
pokuwa mwenye nguvu.[l]

SURA 12

a Eze 8:3
b Eze 3:14
c Efe 1:3
d 2Ko 11:30
e 2Ko 10:8
2Ko 11:16
f Met 16:18
g Ga 4:13
h 1Pe 5:7
i Kum 3:26
j Isa 40:29
Ebr 11:34
k 2Ko 11:30
l Flp 4:13

Safu ya 2

a 2Ko 12:1
b 2Ko 11:5
Ufu 2:2
c 2Ko 11:23
d 1Ko 9:2
e 2Ko 6:4
f Mdo 14:3
Mdo 15:12
Ro 15:19
g 1Ko 9:12
2Ko 11:9
h 2Ko 13:1
i Mdo 20:33
j 1Ko 4:14
Ga 4:19
k Met 13:22
Met 19:14
l Met 11:30
2Ko 1:6
Flp 2:17
Kol 1:24
1Th 2:8
Ebr 13:17
m 2Ko 11:9
n 2Ko 7:2
o 2Ko 8:6
2Ko 8:16
p Flp 1:27

11 Nimekuwa mtu asiye na
akili. Ninyi mlinilazimisha[a]
kuwa hivyo, kwa maana ni-
nyi mlipaswa kunipendekeza.
Kwa maana hata katika jambo
moja sikuwa mdogo kwa mitu-
me wenu walio bora sana,[b] hata
kama mimi si kitu.[c] **12** Kwa
kweli, ishara za mtume[d] zilito-
kezwa katikati yenu kwa uvu-
milivu wote,[e] na kwa ishara na
mambo ya ajabu na matendo ye-
nye nguvu.[f] **13** Kwa maana ni
katika jambo gani kwamba ni-
nyi mlikuwa wadogo kuliko yale
makutaniko mengine, isipoku-
wa kwamba mimi mwenyewe si-
kuwa mzigo kwenu?[g] Mnisame-
he kosa hili kwa fadhili.

14 Tazama! Hii ndiyo mara
ya tatu[h] niliyo tayari kuja kwe-
nu, na bado sitakuwa mzigo.
Kwa maana ninatafuta, si mali
zenu,[i] bali ninyi; kwa maana wa-
toto[j] hawapaswi kuweka akiba
kwa ajili ya wazazi wao, bali wa-
zazi kwa ajili ya watoto wao.[k]
15 Kwa upande wangu mimi ni-
tatumia kwa furaha zaidi na
kutumiwa kabisa kwa ajili ya
nafsi zenu.[l] Kama nikiwapenda
ninyi kwa wingi zaidi, je, mimi
nipendwe kidogo? **16** Lakini
hata iweje, mimi sikuwa mzi-
go mzito kwenu.[m] Hata hivyo
ninyi mnasema, mimi nilikuwa
"mjanja" nami niliwashika
ninyi "kwa ujanja."[n] **17** Kwa
habari ya yeyote kati ya wale
niliowatuma kwenu, je, niliwa-
tumia ninyi kwa kujifaidi kupi-
tia yeye? **18** Nilimhimiza Tito
na nikamtuma yule ndugu pa-
moja naye. Je, Tito aliwatu-
mia ninyi kwa kujifaidi hata ki-
dogo?[o] Je, hatukutembea kati-
ka roho ileile?[p] Katika hatua
zilezile?

19 Je, ninyi mmekuwa mkifikiri muda huu wote kwamba sisi tumekuwa tukijitetea kwenu? Sisi tunasema mbele za Mungu kuhusiana na Kristo. Lakini, wapendwa, mambo yote ni kwa ajili ya kuwajenga ninyi.[a] **20** Kwa maana naogopa kwamba kwa njia fulani, nitakapofika,[b] huenda nikawapata ninyi mkiwa vile ambavyo mimi sipendi nami niwe kwenu vile ambavyo ninyi hampendi, bali, badala yake, kwa njia fulani inaelekea kutakuwa na mizozo, wivu,[c] milipuko ya hasira, magomvi, masengenyo, manong'onezo, majivuno, machafuko.[d] **21** Labda, nitakapokuja tena, huenda Mungu wangu akaninyenyekeza katikati yenu, nami huenda nikaomboleza juu ya wengi kati ya wale ambao hapo zamani walitenda dhambi[e] lakini hawajatubu kutokana na unajisi wao na uasherati[f] na mwenendo mpotovu[g] ambao wamezoea kutenda.

13 Hii ndiyo mara ya tatu[h] ambayo ninakuja kwenu. "Kwa kinywa cha mashahidi wawili au cha watatu kila jambo litathibitishwa."[i] **2** Nimesema hapo mwanzoni na, kana kwamba nipo mara ya pili lakini sipo sasa, nawaambia kimbele wale ambao wametenda dhambi hapo mwanzoni na kwa wengine wote, kwamba ikiwa nitakuja tena sitahurumia,[j] **3** kwa kuwa mnatafuta uthibitisho wa Kristo akisema ndani yangu,[k] Kristo ambaye si dhaifu kuwaelekea ninyi bali ni mwenye nguvu kati yenu. **4** Ni kweli, yeye alitundikwa mtini[l] kwa sababu ya udhaifu,[m] lakini yeye yuko hai kwa sababu ya nguvu za Mungu.[n] Ni kweli, pia, sisi ni dhaifu pamoja naye,[a] lakini tutaishi pamoja naye kwa sababu ya nguvu za Mungu[b] kuwaelekea ninyi.

5 Endeleeni kujijaribu kama ninyi mko katika imani, endeleeni kuthibitisha ninyi wenyewe jinsi mlivyo.[c] Au je, hamtambui kwamba Yesu Kristo yumo katika muungano pamoja na ninyi?[d] Isipokuwa muwe mmekataliwa. **6** Kwa kweli natumaini mtajua kwamba sisi hatujakataliwa.

7 Basi tunasali[e] kwa Mungu kwamba msifanye kosa, si kwamba sisi wenyewe tuonekane kuwa waliokubaliwa, bali kwamba muwe mkifanya yaliyo mazuri, ingawa sisi wenyewe huenda tukaonekana kuwa waliokataliwa. **8** Kwa maana hatuwezi kufanya jambo lolote kinyume cha kweli, bali kwa ajili ya kweli.[f] **9** Hakika sisi hushangilia wakati wowote tunapokuwa dhaifu lakini ninyi ni wenye nguvu;[g] nasi tunasali[h] kwa ajili ya jambo hili, mrekebishwe upya. **10** Hiyo ndiyo sababu naandika mambo haya nikiwa sipo, ili, nitakapokuwapo, nisitende kwa ukali[i] kulingana na mamlaka ambayo Bwana alinipa, ili kujenga[j] na si kubomoa.

11 Mwishowe, akina ndugu, endeleeni kushangilia, kurekebishwa upya, kufarijiwa,[k] kufikiri kwa upatano,[l] kuishi kwa amani;[m] na Mungu wa upendo na wa amani[n] atakuwa pamoja nanyi. **12** Salimianeni kwa busu takatifu.[o] **13** Watakatifu wote wanawatumia ninyi salamu zao.

14 Fadhili zisizostahiliwa za Bwana Yesu Kristo na upendo wa Mungu na ushirika katika roho takatifu ziwe pamoja na ninyi nyote.[p]

SURA 12
a 1Ko 10:33
b 2Ko 10:2
2Ko 13:2
c 1Ko 3:3
d Flp 2:3
e 1Ko 5:1
2Ko 2:2
f 1Ko 6:9
1Ko 6:13
g Ro 13:13
Ga 5:19
Efe 4:19
2Pe 2:2
Yud 4

SURA 13
h 2Ko 12:14
i Hes 35:30
Kum 19:15
Mt 18:16
Yoh 8:17
j 2Ko 1:23
2Ko 10:2
2Ko 12:21
k Ro 15:18
1Ko 5:4
l 1Ko 2:2
m Flp 2:7
n Ro 6:4

Safu ya 2
a 2Ti 2:12
1Pe 3:18
b 1Ko 1:18
1Ko 6:14
c 1Ko 11:28
Ga 6:4
d Ro 8:10
e Ro 1:9
Flp 1:4
Flp 1:9
Kol 1:3
1Th 1:2
f Mdo 4:20
1Ko 13:6
g 1Ko 4:10
h 1Th 3:10
i 1Ko 4:21
2Ko 10:6
j Tit 1:13
k 2Ko 1:4
2Ko 1:6
l Flp 2:2
m 1Th 5:13
Yak 3:17
1Pe 3:11
2Pe 3:14
n Ro 15:33
1Ko 14:33
1Th 5:23
o Ro 16:16
1Th 5:26
1Pe 5:14
p Flp 2:1

KWA

WAGALATIA

1 Paulo,[a] mtume,[b] si kutokana na wanadamu wala kupitia mwanadamu fulani, bali
kupitia Yesu Kristo[c] na Mungu
Baba,[d] aliyemfufua yeye kutoka
kwa wafu,[e] **2** na ndugu wote
walio pamoja nami,[f] kwa maku-
taniko ya Galatia:[g]
3 Na muwe na fadhili zisizo-
stahiliwa na amani[h] kutoka kwa
Mungu Baba yetu na Bwana
Yesu Kristo. **4** Alijitoa mwe-
nyewe kwa ajili ya dhambi zetu[i]
ili atukomboe kutoka katika
mfumo mwovu wa mambo[j] wa
sasa, kulingana na mapenzi[k] ya
Mungu na Baba yetu, **5** kwake
kuwe na utukufu milele na mile-
le.[l] Amina.
6 Mimi ninashangaa kwa-
mba mnaondolewa upesi hivyo
kutoka kwake Yeye[m] aliyewai-
ta ninyi kwa fadhili zisizosta-
hiliwa[n] za Kristo nanyi mna-
pelekwa kwenye habari nje-
ma ya aina nyingine.[o] **7** La-
kini si nyingine; isipokuwa tu
kuna watu fulani wanaowataa-
bisha[p] ninyi na kutaka kupoto-
sha habari njema juu ya Kristo.[q]
8 Lakini, hata ikiwa sisi au ma-
laika kutoka mbinguni tunge-
watangazia ninyi kuwa habari
njema jambo fulani kupita lile
tulilowatangazia ninyi kuwa ha-
bari njema, mtu huyo na alaani-
we.[r] **9** Kama vile tulivyosema
hapo juu, sasa mimi pia nase-
ma tena, Mtu yeyote anayewata-
ngazia ninyi jambo fulani kupi-
ta lile mlilopokea[s] kuwa hilo ni
habari njema, na alaaniwe.
10 Kwa kweli, je, sasa ni-
najaribu kushawishi wanada-
mu au Mungu? Au je, ninata-
futa kuwapendeza wanadamu?[a]
Kama ningekuwa bado nina-
wapendeza wanadamu,[b] mimi si-
ngekuwa mtumwa[c] wa Kristo.
11 Kwa maana nawajulisha ni-
nyi, akina ndugu, kwamba ha-
bari njema ambayo niliitangaza
kuwa habari njema si jambo
la kibinadamu;[d] **12** kwa maa-
na sikuipokea kutoka kwa mwa-
nadamu, wala sikufundishwa
hiyo, isipokuwa kupitia ufunuo
wa Yesu Kristo.[e]
13 Bila shaka, ninyi mlisikia
juu ya mwenendo wangu hapo
zamani katika dini ya Kiyahu-
di,[f] kwamba kufikia hatua ya
kuzidi mno niliendelea kulite-
sa[g] kutaniko la Mungu na ku-
liangamiza,[h] **14** nami nilikuwa
nikifanya maendeleo ma-
kubwa zaidi katika dini ya Ki-
yahudi kuliko watu wengi wa
umri wangu katika jamii yangu,[i]
kwa kuwa nilikuwa mwenye bi-
dii zaidi[j] kwa ajili ya mapokeo[k]
ya baba zangu. **15** Lakini wa-
kati Mungu, aliyenitenga mimi
tangu tumbo la uzazi la mama
yangu na kuniita[l] kupitia fadhi-
li zake zisizostahiliwa,[m] alipoo-
na vema **16** kumfunua Mwa-
na wake kuhusiana nami,[n] ili ni-
tangaze habari njema juu yake
kwa mataifa,[o] mimi sikuingia
mara moja katika mashauria-
no pamoja na watu wenye mwili
na damu.[p] **17** Wala sikupanda
kwenda Yerusalemu kwa wale
waliokuwa mitume kabla ya-
ngu,[q] bali nilienda nikaingia
Arabia, nami nikarudi tena Da-
masko.[r]

SURA 1

a Mdo 13:9
b Ro 1:5
Tit 1:1
c Mdo 9:15
Mdo 26:16
Ga 1:12
d Mdo 22:14
e Mdo 2:24
f Flp 4:21
g 1Ko 16:1
h 1Ko 1:3
Ga 6:16
2Yo 3
i Tit 2:14
1Yo 2:2
j Yoh 15:19
Ro 12:2
k Eze 33:11
1Ti 2:4
l Ro 16:27
m Ebr 3:6
n 2Ko 1:2
o 2Ko 11:4
Ga 5:7
p Ga 5:10
q Mdo 15:1
2Ko 11:13
1Ti 6:3
r 1Ko 16:22
Ga 5:12
s Kum 12:32
Met 30:6

Safu ya 2

a 1Th 2:4
b Yak 4:4
c Ro 1:1
d 1Th 2:13
e Ro 16:25
Ga 2:2
Efe 3:3
f Mdo 23:6
Ga 2:14
g 1Ti 1:13
h Mdo 8:3
Mdo 9:1
Mdo 22:4
Mdo 26:11
i Mdo 22:3
j Flp 3:6
k Mk 7:5
l 1Ko 1:1
1Th 2:12
m Ro 11:5
1Ko 15:10
Efe 3:7
n 2Ko 4:6
o Mdo 9:15
Ro 11:13
p Mt 16:17
q Mdo 2:42
r Mdo 9:19

18 Kisha miaka mitatu baadaye nilipanda kwenda Yerusalemu[a] kumtembelea Kefa,[b] nami
nikakaa pamoja naye siku kumi
na tano. **19** Lakini sikuona
mwingine yeyote wa wale mi-
tume, isipokuwa Yakobo[c] ndu-
gu[d] ya Bwana. **20** Sasa kuhu-
su mambo ninayowaandikia ni-
nyi, tazameni! machoni pa Mu-
ngu, mimi sisemi uwongo.[e]
21 Baada ya hayo nilienda[f]
katika maeneo ya Siria na ya
Kilikia. **22** Lakini mimi siku-
julikana kwa uso kwa makuta-
niko ya Yudea yaliyokuwa ka-
tika muungano na Kristo;[g]
23 yalikuwa tu yakisikia: "Yule
mtu ambaye hapo zamani ali-
tutesa[h] sasa anaitangaza ha-
bari njema juu ya imani amba-
yo hapo zamani aliiangamiza."[i]
24 Kwa hiyo wakaanza kumtu-
kuza[j] Mungu kwa sababu yangu.

2 Kisha baada ya miaka kumi
na minne nilipanda tena
kwenda Yerusalemu[k] pamoja na
Barnaba,[l] nikichukua pia Tito
pamoja nami. **2** Lakini nilipa-
nda kwenda kutokana na ufu-
nuo.[m] Nami nikaweka mbele
yao[n] habari njema ambayo nina-
hubiri kati ya mataifa, hata hi-
vyo, kwa faragha, mbele ya wale
waliokuwa watu wenye kutoke-
za, ili isije kuwa kwamba kwa
njia fulani nilikuwa ninakimbia[o]
au nilikuwa nimekimbia bure.[p]
3 Lakini, hata Tito,[q] aliyekuwa
pamoja nami, hakulazimishwa
kutahiriwa,[r] ijapokuwa aliku-
wa Mgiriki. **4** Lakini kwa sa-
babu ya akina ndugu wa uwo-
ngo[s] walioingizwa ndani kimya-
kimya,[t] walioingia kisirisiri ili
kupeleleza uhuru[u] wetu tulio
nao katika muungano na Kristo
Yesu, ili watufanye sisi kuwa wa-
tumwa[a] kabisa— **5** kwa hao
sisi hatukuwaachia nafasi kwa
kujitiisha,[b] hapana, hata kwa
saa moja, ili kweli[c] ya haba-
ri njema iendelee kuwa pamo-
ja nanyi.
6 Lakini kwa upande wa
wale walioonekana kuwa ni
kitu[d]—hata kama walikuwa
watu wa namna gani hapo za-
mani haileti tofauti yoyote
kwangu[e]—Mungu hafuati sura
ya nje[f] ya mwanadamu—kwa-
ngu, kwa kweli, hao watu wenye
kutokeza hawakunipa jambo
lolote jipya. **7** Bali, kinyume
chake, walipoona kwamba nili-
kuwa nimekabidhiwa[g] habari
njema kwa ajili ya wale wasiota-
hiriwa,[h] kama vile Petro alivyo-
kuwa nayo kwa ajili ya wale wa-
liotahiriwa[i]— **8** kwa maana
Yeye aliyempa Petro nguvu zi-
nazohitajika kwa ajili ya utume
kwa wale waliotahiriwa alini-
pa mimi pia nguvu[j] kwa ajili ya
wale walio wa mataifa; **9** ndi-
yo, walipokuja kujua fadhili zi-
sizostahiliwa[k] nilizopewa,[l] Yako-
bo[m] na Kefa na Yohana, wale wa-
lioonekana kuwa nguzo,[n] wali-
nipa mimi na Barnaba[o] mkono
wa kuume wa kushirikiana pa-
moja,[p] ili sisi twende kwa mataifa, bali wao waende kwa wale waliotahiriwa. **10** Ila sisi tuwakumbuke walio maskini.[q] Jambo hili mimi pia nimejitahidi sana kulifanya.[r]

11 Hata hivyo, Kefa[s] alipokuja Antiokia,[t] nilimpinga uso kwa uso, kwa sababu alistahili kuhukumiwa hatia.[u] **12** Kwa maana kabla ya kufika kwa watu fulani kutoka kwa Yakobo,[v] alikuwa akila[w] chakula pamoja na watu wa mataifa; lakini walipofika, akaanza kujiondoa na

SURA 1

a Mdo 9:26
b Yoh 1:42
1Ko 15:5
c Mdo 12:17
d Mt 13:55
1Ko 9:5
e Ro 9:1
f Mdo 9:30
g Yoh 17:21
Ro 16:7
1Ko 1:30
1Th 2:14
h Ga 1:13
i Mdo 8:3
j Mdo 21:20

SURA 2

k Mdo 15:2
l Mdo 9:27
m 1Ko 14:6
n Mdo 15:12
o Ga 5:7
p Flp 2:16
1Th 3:5
q 2Ko 2:13
r Mdo 16:3
s Isa 66:5
t Mdo 15:24
2Ko 11:26
Yud 4
u Yoh 8:32
Yoh 8:36
2Ko 3:17
Ga 5:1
1Pe 2:16

Safu ya 2

a 2Ko 11:20
Ga 4:9
b Ga 2:14
c Yoh 18:37
Ga 4:16
d Ga 2:9
e Ga 2:14
f Kum 10:17
Mdo 10:34
Ro 2:11
g 1Th 2:4
h Mdo 22:21
Ro 11:13
1Ti 2:7
i Mdo 8:14
j Mdo 9:15
Ro 1:5
Kol 1:29
k Ro 1:5
Efe 3:8
l 2Pe 3:15
m Mdo 15:13
n Efe 2:20
o Mdo 13:2
Mdo 15:25
p 1Yo 1:3
q Kum 15:8
1Ko 16:1
r Mdo 11:29
s Yoh 1:42
t Mdo 11:26
Mdo 15:35
u Law 19:17
v Mdo 12:17
w Mdo 10:28
Mdo 11:3
Mdo 15:28

kujitenga mwenyewe, kwa kuwaogopa[a] hao wa jamii ya waliotahiriwa.[b] **13** Wale Wayahudi wengine pia walijiunga naye katika kufanya unafiki[c] huo, hivi kwamba hata Barnaba[d] akaongozwa pamoja nao katika unafiki wao. **14** Lakini nilipoona kwamba hawakuwa wakitembea kwa unyoofu kulingana na kweli ya habari njema,[e] nilimwambia Kefa mbele yao wote:[f] "Ikiwa wewe, ingawa ni Myahudi, unaishi kama vile mataifa wanavyoishi, na si kama Wayahudi wanavyoishi, kwa nini wewe unawalazimisha watu wa mataifa kuishi kulingana na mazoea ya Kiyahudi?"[g]

15 Sisi tulio Wayahudi kwa asili,[h] na si watenda-dhambi[i] kutoka kwa mataifa, **16** tukijua kama vile tunavyojua kwamba mtu hutangazwa kuwa mwadilifu,[j] si kwa sababu ya matendo ya sheria, bali tu kupitia imani[k] kumwelekea Kristo Yesu, hata sisi tumeweka imani yetu katika Kristo Yesu, ili tutangazwe kuwa waadilifu kutokana na imani kumwelekea Kristo,[l] na si kutokana na matendo ya sheria, kwa sababu hakuna mwili wowote utakaotangazwa kuwa mwadilifu kutokana na matendo ya sheria.[m] **17** Basi ikiwa sisi, katika kutafuta kutangazwa kuwa waadilifu kwa njia ya Kristo,[n] sisi wenyewe pia tumepatikana kuwa watenda-dhambi,[o] je, Kristo kwa kweli ni mhudumu wa dhambi?[p] Hilo lisitendeke kamwe! **18** Kwa maana ikiwa ninayajenga tena yale mambo ambayo wakati mmoja niliyabomoa,[q] mimi najionyesha mwenyewe kuwa mkosaji.[r] **19** Kwa habari yangu, kupitia sheria nilikufa kuielekea sheria,[a] ili niwe hai kumwelekea Mungu.[b] **20** Mimi nimetundikwa mtini pamoja na Kristo.[c] Si mimi tena niliye hai,[d] bali Kristo ndiye anayeishi katika muungano na mimi.[e] Kwa kweli, uhai ninaoishi sasa[f] katika mwili naishi kwa imani ambayo ni kumwelekea Mwana wa Mungu, aliyenipenda mimi na kujitoa mwenyewe kwa ajili yangu.[g] **21** Mimi sizitupi fadhili zisizostahiliwa za Mungu;[h] kwa maana ikiwa uadilifu ni kupitia sheria,[i] Kristo kwa kweli alikufa bure tu.[j]

3 Enyi Wagalatia wasio na akili, ni nani huyo aliyewaleta chini ya uvutano mwovu,[k] ninyi ambao machoni penu Yesu Kristo alionyeshwa waziwazi akiwa ametundikwa mtini?[l] **2** Nataka kujifunza hili peke yake kutoka kwenu: Je, mlipokea roho[m] kutokana na matendo ya sheria[n] au kutokana na kusikia[o] kwa njia ya imani? **3** Je, ninyi hamna akili kabisa? Baada ya kuanza katika roho,[p] je, sasa mnamalizia katika mwili?[q] **4** Je, mlipatwa na mateso mengi sana bila kusudi?[r] Ikiwa kwa kweli ilikuwa bila kusudi lolote. **5** Kwa hiyo, yeye anayewapa ninyi roho[s] na kufanya matendo yenye nguvu[t] katikati yenu, je, yeye hufanya hivyo kutokana na matendo ya sheria au kutokana na kusikia kwa njia ya imani? **6** Kama vile Abrahamu "alivyokuwa na imani katika Yehova, na ikahesabiwa kwake kuwa ni uadilifu."[u]

7 Hapana shaka mnajua kwamba wale wanaoshikamana na imani[v] ndio wale walio wana wa Abrahamu.[w] **8** Sasa Andiko, likitangulia kuona kwamba

SURA 2

a Met 29:25
b Mdo 21:20
c Yak 3:17
d Mdo 15:39
e Mdo 10:15
Mdo 10:34
Ga 3:28
f 1Ti 5:20
g Mdo 15:10
Mdo 15:28
Ga 1:13
h Yoh 8:39
Ro 11:23
i Efe 2:12
j Zb 143:2
Mdo 13:39
Ro 8:33
k Ro 1:17
Ro 3:22
Yak 2:23
l Ro 5:17
1Ko 6:11
Ebr 7:19
m Ro 3:20
Ga 3:19
n Ro 5:1
o 1Yo 3:9
p Ro 6:1
q Ga 5:2
Kol 2:14
r Ga 5:4

Safu ya 2

a Ro 7:9
b Ro 6:11
Ebr 9:14
c Ro 6:6
Ga 5:24
Ga 6:14
d 1Pe 4:2
e Yoh 17:23
f 2Ko 5:15
g 1Ti 2:6
h Yoh 1:17
Ro 4:5
i Ga 3:21
Ebr 7:11
j Tit 3:5

SURA 3

k Ga 5:7
l 1Ko 1:23
m Efe 1:13
Ebr 6:4
n Ro 3:20
o Ro 10:17
p Ga 4:9
q Ebr 7:16
r Ebr 10:36
2Yo 8
s Mdo 10:44
t 1Ko 12:10
u Mwa 15:6
Ro 4:3
Yak 2:23
v Ro 4:12
w Yoh 8:39
Ro 4:16

Mungu atawatangaza watu wa
mataifa kuwa waadilifu kutokana na imani, lilitangaza habari
njema kimbele kwa Abrahamu,
yaani: "Kupitia kwako mataifa
yote yatabarikiwa."[a] **9** Kwa
sababu hiyo wale wanaoshi-
kamana na imani wanabariki-
wa[b] pamoja na Abrahamu mwa-
minifu.[c]

10 Kwa maana wote wana-
otegemea matendo ya sheria
wako chini ya laana; kwa ma-
ana imeandikwa: "Amelaani-
wa kila mtu asiyedumu katika
mambo yote yaliyoandikwa ka-
tika kitabu cha kukunjwa cha
Sheria ili ayafanye."[d] **11** Tena,
kwamba hakuna yeyote amba-
ye kwa njia ya sheria hutanga-
zwa kuwa mwadilifu[e] kwa Mu-
ngu ni wazi, kwa maana "mwa-
dilifu ataishi kwa sababu ya
imani."[f] **12** Sasa Sheria hai-
shikamani na imani, bali "yeye
anayezifanya ataishi kwa hizo."[g]
13 Kristo kwa kutununua[h] ali-
tuachilia huru[i] kutoka katika la-
ana ya Sheria kwa yeye kuwa
laana[j] badala yetu, kwa sababu
imeandikwa: "Amelaaniwa kila
mtu aliyetundikwa juu ya mti."[k]
14 Kusudi lilikuwa kwamba ba-
raka ya Abrahamu ije kupitia
Yesu Kristo kwa ajili ya matai-
fa,[l] ili tuipokee roho iliyoahidi-
wa[m] kupitia imani yetu.[n]

15 Akina ndugu, nasema kwa
njia ya mfano wa mwanadamu:
Agano lililohalalishwa, ingawa ni
la mwanadamu, hakuna yeyote
anayelifuta au kuongeza jambo
juu yake.[o] **16** Sasa ahadi zilito-
lewa kwa Abrahamu[p] na kwa
uzao wake.[q] Haisemi: "Na kwa
wazao," kana kwamba ni we-
ngi wa namna hiyo, bali kana
kwamba ni mmoja:[r] "Na kwa
uzao wako,"[a] ambaye ni Kri-
sto.[b] **17** Zaidi, mimi nasema
hivi: Kuhusu agano lililohalali-
shwa na Mungu[c] hapo kwanza,
Sheria ambayo imekuja kuwapo
miaka 430[d] baadaye hailitangui,
ili kuifuta ahadi.[e] **18** Kwa ma-
ana ikiwa urithi ni kutokana na
sheria, hautokani tena na ahadi;[f]
lakini Mungu amempa huo
Abrahamu kwa fadhili kupitia
ahadi.[g]

19 Basi, kwa nini Sheria? Ili-
ongezwa ili kufanya makosa
yawe wazi,[h] mpaka ufike uzao[i]
ambao ulikuwa umepewa aha-
di; na ilipitishwa kupitia malai-
ka[j] kwa mkono wa mpatanishi.[k]
20 Sasa hakuna mpatanishi ma-
hali ambapo ni mtu mmoja tu
anayehusika, lakini Mungu ni
mmoja tu.[l] **21** Kwa hiyo, je,
Sheria inapinga ahadi za Mu-
ngu?[m] Hilo na lisitendeke ka-
mwe! Kwa maana kama ingali-
tolewa sheria inayoweza ku-
toa uhai,[n] kwa kweli uadilifu
ungalikuwa kwa njia ya sheria.[o]
22 Lakini Andiko[p] liliyafunga
mambo yote pamoja katika kifu-
ngo cha dhambi,[q] ili ahadi ina-
yotokana na imani kumwelekea
Yesu Kristo ipewe wale wanaoa-
mini.[r]

23 Hata hivyo, kabla ya ile
imani kufika,[s] tulikuwa tukili-
ndwa chini ya sheria,[t] tukiwe-
kwa pamoja kifungoni, tukii-
tazamia imani iliyokusudiwa ku-
funuliwa.[u] **24** Kwa sababu hiyo
Sheria imekuwa mtunzaji wetu
kutuongoza kwa Kristo,[v] ili tu-
tangazwe kuwa waadilifu[w] kuto-
kana na imani. **25** Lakini sasa
kwa kuwa imani imefika,[x] sisi ha-
tuko tena chini ya mtunzaji.[y]

SURA 3
a Mwa 12:3 Mwa 18:18 Mdo 3:25
b Ebr 13:7
c Ga 3:28 Ga 3:29 Ebr 2:16
d Kum 27:26 Yer 11:3 Mdo 15:10 Yak 2:10
e Mdo 13:39 Ga 2:16
f Hab 2:4 Ebr 10:38
g Law 18:5 Kum 30:16 Ne 9:29 Ro 10:5
h 1Ko 7:23
i Isa 35:10 Mt 26:28 Tit 2:14 Ebr 9:15
j Hes 21:9 Yoh 3:14 Yoh 19:31 Mdo 5:30
k Kum 21:23
l Ro 4:9 Efe 2:15
m Yoe 2:28
n Mdo 19:4 1Pe 2:6
o Ebr 9:17
p Mwa 12:1 Mwa 12:7 Mwa 13:15 Mwa 17:7
q Mwa 24:7 Isa 6:13 Ga 3:29
r Mwa 25:5 Ro 9:7 Ro 9:8

Safu ya 2
a Mwa 22:18
b Mwa 49:10 Mt 1:17
c Ro 4:13
d Kut 12:41
e Ro 4:14
f Ro 11:6
g Mwa 22:17
h Ro 3:20 Ro 4:15 Ro 7:12 Ro 7:14
i Yoh 1:29 Ro 10:4
j Mdo 7:38 Mdo 7:53 Ebr 2:2
k Kut 20:19 Kum 5:5 Yoh 1:17 Ebr 9:15
l Kum 6:4
m 1Ti 1:8
n Ro 8:3
o Ro 3:10 Ga 2:21
p Mt 11:13
q Ro 3:9
r Ro 4:11
s Ga 4:4
t Kol 2:14
u Ro 10:4
v Mt 5:17 Ebr 8:5
w Mdo 13:39; Ro 5:1; Ro 8:33; x Kol 2:17; y Mdo 21:21; Ebr 8:6; Ebr 10:1.

26 Ninyi nyote, kwa kweli,
ni wana[a] wa Mungu kupitia
imani yenu katika Kristo Yesu.
27 Kwa maana ninyi nyote mli-
obatizwa katika Kristo[b] mme-
mvaa Kristo.[c] **28** Hakuna
Myahudi wala Mgiriki,[d] hakuna
mtumwa wala mtu huru,[e] haku-
na mwanamume wala mwana-
mke;[f] kwa maana ninyi nyote
ni mtu mmoja katika muunga-
no na Kristo Yesu.[g] **29** Zaidi
ya hayo, ikiwa ninyi ni wa Kri-
sto, ninyi kwa kweli ni uzao wa
Abrahamu,[h] warithi kuhusiana
na ahadi.[i]

4 Basi nasema kwamba waka-
ti mrithi anapokuwa anga-
li mtoto mchanga hatofautiani
hata kidogo na mtumwa,[j] inga-
wa yeye ni bwana wa vitu vyo-
te, **2** bali yeye yuko chini ya
watu wenye kusimamia[k] na chi-
ni ya wasimamizi-nyumba mpa-
ka siku ambayo baba yake ali-
iweka kimbele. **3** Vivyo hivyo
sisi pia, tulipokuwa watoto wa-
changa, tuliendelea kutumiki-
shwa na mambo ya msingi[l] ya-
liyo ya ulimwengu. **4** Lakini
wakati kamili ulipofika,[m] Mu-
ngu alimtuma Mwana wake,[n] ali-
yezaliwa na mwanamke[o] na ali-
yekuja kuwa chini ya sheria,[p]
5 ili awaachilie huru kwa kuwa-
nunua[q] wale walio chini ya she-
ria,[r] ili sisi nasi tufanywe kuwa
wana.[s]

6 Sasa kwa sababu ninyi ni
wana, Mungu ametuma roho[t]
ya Mwana wake ndani ya mi-
oyo yetu nayo hupaaza sauti:
"Abba, Baba!"[u] **7** Basi, wewe
si mtumwa tena bali ni mwana;
na ikiwa ni mwana, pia ni mrithi
kupitia Mungu.[v]

8 Hata hivyo, wakati hamku-
mjua Mungu,[w] ndipo mlipoi-

SURA 3

a Ho 1:10
Yoh 1:12
Ro 8:14
b Mdo 19:5
Ro 6:3
c Ro 13:14
Efe 4:24
d Ro 10:12
e 1Ko 12:13
Kol 3:11
f Mdo 2:17
1Pe 3:7
g Yoh 17:21
h Isa 54:1
Ro 8:17
Ro 9:7
i Ga 4:28

SURA 4

j Lu 2:51
k Mwa 24:3
l Kol 2:8
Ebr 9:10
m Mwa 3:15
Mwa 49:10
n Mt 3:17
Yoh 8:42
o Yoh 1:14
1Ti 3:16
Ebr 2:14
p Mt 5:17
q 1Ko 7:23
Ga 3:13
r Mt 20:28
s Yoh 1:12
Ro 8:23
2Ko 6:18
t Yoh 14:26
Ro 5:5
u Mk 14:36
Ro 8:15
v Ro 8:17
Ga 3:29
Efe 1:14
w Efe 2:12
1Th 4:5

Safu ya 2

a Ro 1:25
1Ko 12:2
1Th 1:9
b 1Ko 8:3
c Kol 2:20
d Ro 8:3
Ebr 7:18
e 2Ko 11:20
f Ro 14:5
g Kol 2:16
h Ga 2:2
Ga 3:4
1Th 3:5
i Ga 6:14
j Ga 1:14
k 2Ko 2:5
l Mdo 16:6
m 2Sa 19:27
n Mt 10:40
Yoh 13:20
o Ufu 2:4
p Ga 6:11
q Met 27:6
Isa 63:10
Ebr 12:6
r Yoh 8:45
Efe 4:15
s Ro 16:18
2Pe 2:3
2Pe 2:18
t Mdo 20:30
Flp 2:21
u 1Ko 15:58
Tit 2:14
v Flp 2:12

tumikia ile ambayo kwa asili
si miungu.[a] **9** Lakini sasa kwa
kuwa mmemjua Mungu, au afa-
dhali zaidi kwamba sasa Mu-
ngu amewajua ninyi,[b] kwa nini
mnarudi tena kwenye mambo
ya msingi[c] yaliyo dhaifu[d] na ya-
siyo na maana na kutaka ku-
yatumikia kwa mara nyingine
tena?[e] **10** Mnashika kwa ua-
ngalifu mwingi siku[f] na miezi[g]
na majira na miaka. **11** Mimi
naogopa kwa ajili yenu, isiwe
kwamba kwa njia fulani nimeji-
taabisha kwa ajili yenu bila ku-
sudi[h] lolote.

12 Akina ndugu, ninawa-
omba ninyi, Iweni kama nili-
vyo,[i] kwa sababu mimi nilikuwa
pia kama mlivyo.[j] Hamkunite-
ndea kosa lolote.[k] **13** Lakini
mnajua kwamba ilikuwa
kupitia ugonjwa wa mwili wa-
ngu kwamba niliwatangazia ni-
nyi habari njema mara ya kwa-
nza.[l] **14** Na lililokuwa jaribu
kwenu katika mwili wangu, ha-
mkulitendea kwa dharau au
kulitemea mate kwa chuki;
bali mlinipokea kama malaika[m]
wa Mungu, kama Kristo
Yesu.[n] **15** Basi, iko wapi ile fu-
raha mliyokuwa nayo?[o] Kwa
maana nawatolea ninyi ushahi-
di kwamba, kama ingaliwezeka-
na, mngaling'oa macho yenu na
kunipa hayo.[p] **16** Hivyo basi,
je, nimekuwa adui[q] yenu kwa
sababu nawaambia ninyi kwe-
li?[r] **17** Wao wanawatafuta ni-
nyi kwa bidii,[s] si kwa uzuri,
bali wanataka kuwazuia ninyi
kutoka kwangu, ili mwatafu-
te wao kwa bidii.[t] **18** Hata hi-
yo, ni vema kwenu mkitafu-
twa kwa bidii kwa kusudi zuri[u]
nyakati zote, na si wakati tu
mimi ninapokuwa pamoja na-
nyi,[v] **19** watoto wangu wado-

go,[a] ambao tena nina maumivu
ya kuwazaa mpaka Kristo au-
mbike ndani yenu.[b] **20** Lakini
ningependa kuwa pamoja nanyi
sasa hivi[c] na kusema kwa njia
tofauti, kwa sababu nahangaika[d] juu yenu.

21 Mniambie, ninyi mnaota-
ka kuwa chini ya sheria,[e] Je, ha-
msikii Sheria?[f] **22** Kwa mfa-
no, imeandikwa kwamba Abra-
hamu alipata wana wawili,
mmoja kwa njia ya kijakazi[g] na
mmoja kwa njia ya mwanamke
huru;[h] **23** lakini yule wa kija-
kazi kwa kweli alizaliwa kati-
ka namna ya mwili,[i] yule mwi-
ngine wa mwanamke huru ku-
pitia ahadi.[j] **24** Mambo haya
yanasimama yakiwa tukio la
mfano;[k] kwa maana wanawake
hawa wanamaanisha maagano
mawili,[l] moja kutoka Mlima Si-
nai,[m] ambalo huzaa watoto kwa
ajili ya utumwa, na ambalo ni
Hagari. **25** Basi Hagari huyu
anamaanisha Sinai,[n] mlima ulio
Arabia, naye analingana na Ye-
rusalemu la leo, kwa maana liko
katika utumwa[o] pamoja na wa-
toto wake. **26** Lakini Yerusa-
lemu[p] la juu liko huru, nalo ni
mama yetu.[q]

27 Kwa maana imeandi-
kwa: "Furahi, wewe mwana-
mke tasa usiyezaa; paaza sauti
na kupaaza kilio kikubwa, wewe
mwanamke ambaye huna mau-
mivu ya kuzaa mtoto; kwa maa-
na watoto wa mwanamke ali-
ye na ukiwa ni wengi kuliko
wale wa yule aliye na mume."[r]
28 Basi, akina ndugu, sisi ni
watoto wa ahadi kama Isaka
alivyokuwa.[s] **29** Lakini kama
ilivyokuwa wakati huo, yule
aliyezaliwa katika namna ya
mwili alianza kumtesa[t] yule
aliyezaliwa katika namna ya
roho, ndivyo ilivyo pia na sasa.[a]
30 Hata hivyo, Andiko linasema nini? "Mfukuze kijakazi na
mwana wake, kwa maana mwa-
na wa kijakazi hatakuwa mri-
thi hata kidogo pamoja na
mwana wa mwanamke huru."[b]
31 Kwa hiyo, akina ndugu, sisi
ni watoto, si wa kijakazi,[c] bali wa
yule mwanamke huru.[d]

5 Kristo alituweka huru[e]
tuwe na uhuru wa namna
hiyo. Kwa hiyo simameni ima-
ra,[f] na msijiache wenyewe kufu-
ngwa tena katika nira ya utu-
mwa.[g]

2 Oneni! Mimi, Paulo, nina-
waambia ninyi kwamba mkita-
hiriwa,[h] Kristo hatakuwa na faida kwenu. **3** Zaidi ya hayo, na-
toa ushahidi tena kwa kila mtu
anayetahiriwa kwamba yuko
chini ya wajibu kuitimiza She-
ria yote.[i] **4** Mmetenganishwa
na Kristo, hata muwe ninyi ni
nani ambao mnajaribu kutanga-
zwa kuwa waadilifu kwa njia
ya sheria;[j] mmeanguka kutoka
kwenye fadhili zake zisizostahi-
liwa.[k] **5** Kwa upande wetu
sisi kwa njia ya roho tunango-
jea kwa hamu uadilifu ulio-
tumainiwa kutokana na imani.[l]
6 Kwa maana kwa habari ya
zitachakaa kama vazi la nje,[h]
12 nawe utazikunja kama ka-
nzu,[i] kama vazi la nje; nazo zita-
badilishwa, lakini wewe ni yu-
leyule, nayo miaka yako haita-
kwisha kamwe."[j]
13 Lakini amepata kusema
hivi kuhusu nani kati ya ma-

SURA 1
a Hes 12:8
Isa 1:2
b Kut 24:3
Yer 7:25
Eze 33:33
Lu 1:70
Mdo 3:21
c Ga 4:4
1Pe 1:11
1Pe 1:20
d Mt 17:5
Yoh 3:17
Yoh 13:34
e Zb 2:8
Yoh 16:15
Ro 8:17
f Yoh 1:3
1Ko 8:6
Kol 1:16
g Yoh 1:14
Yoh 17:5
h Yoh 1:1
Kol 1:15
i Kol 1:17
j Da 9:24
Ebr 9:26
1Pe 1:19
k Zb 110:1
Mdo 2:33
Mdo 7:55
Ro 8:34
Kol 3:1
l Zb 33:13
Efe 1:20
Ebr 8:1
Yud 25
m Efe 1:21
1Pe 3:22
n Mdo 4:12
Flp 2:9
o Zb 2:7
p 2Sa 7:14
Mk 1:11
Lu 9:35
2Pe 1:17
q Yoh 1:14
Yoh 3:18
Ro 8:29
Kol 1:15
r Zb 91:11
Lu 22:43
Yoh 20:12
s Kum 32:43
Zb 97:7

Safu ya 2
a Zb 104:4

b Mt 28:18; Mdo 2:30; Ufu 3:21; c Mwa 49:10; Hes 24:17; Zb 2:9; d Zb 45:6; e Isa 61:1; Lu 3:22; Lu 4:18; Mdo 4:27; Mdo 10:38; f Zb 45:7; g Zb 102:25; h Isa 51:6; i Isa 34:4; Ufu 6:14; j Zb 102:26.

laika: "Keti kwenye mkono wangu wa kuume, mpaka niwaweke adui zako kuwa kiti cha miguu yako"?[a] **14** Je, wao wote si roho[b] kwa ajili ya utumishi wa watu wote,[c] waliotumwa kuhudumu kwa ajili ya wale watakaorithi[d] wokovu?

2 Hiyo ndiyo sababu ni lazima kwetu kuyakazia uangalifu zaidi kuliko ilivyo kawaida mambo tuliyosikia,[e] ili tusipeperushwe kamwe.[f] **2** Kwa maana ikiwa neno lililosemwa kupitia malaika[g] lilikuwa imara, na kila kosa na tendo la kutotii lilipokea malipo kupatana na haki;[h] **3** sisi tutaponaje[i] ikiwa tumepuuza[j] wokovu mkuu[k] namna hii kwa kuwa ulianza kusemwa kupitia Bwana[l] wetu nasi tukathibitishiwa[m] na wale waliomsikia, **4** huku Mungu akijiunga katika kutoa ushahidi kwa ishara na vilevile mambo ya ajabu na matendo mbalimbali yenye nguvu[n] na kwa ugawaji[o] wa roho takatifu kulingana na mapenzi yake?[p]

5 Kwa maana yeye hajaitiisha chini ya malaika dunia yenye kukaliwa inayokuja,[q] ambayo sisi tunasema kuihusu. **6** Bali shahidi fulani ametoa uthibitisho mahali fulani, akisema: "Mwanadamu ni nini hivi kwamba umweke akilini,[r] au mwana wa binadamu hivi kwamba umtunze?[s] **7** Ulimfanya mdogo kidogo kuliko malaika; ulimvika taji kwa utukufu na heshima,[t] na kumweka juu ya kazi za mikono yako.[u] **8** Vitu vyote ulivitiisha chini ya miguu yake."[v] Kwa maana yeye alivitiisha vitu vyote chini yake,[w] Mungu hakuacha kitu chochote kisichotiishwa chini yake.[x]

SURA 1
a Zb 110:1 Mt 22:44 Mk 12:36 Lu 20:42
b Zb 104:4 Mdo 23:8
c Zb 34:7 Zb 91:11 Mt 18:10 Lu 2:9 Lu 2:13 Mdo 5:19 Mdo 12:7
d Mt 19:29 Mt 25:34 Yak 2:5

SURA 2
e Lu 8:15 2Ti 2:2
f Zb 73:2 Ebr 3:12 2Pe 3:17 Ufu 2:4
g Mdo 7:53 Ga 3:19
h Kum 4:3 1Ko 10:11 Yud 5
i Ebr 10:29
j Mt 11:23 Mt 22:5
k Lu 1:69
l Mk 1:14 Yoh 18:20
m Lu 1:2
n Mdo 2:22 1Ko 2:4
o 1Ko 12:4
p 1Ko 12:11 Efe 1:9 Ufu 4:11
q Isa 11:9 Mdo 17:31 2Pe 3:13
r Ayu 7:17
s Zb 8:4 Zb 144:3
t Zb 8:5
u Mwa 1:26 Mwa 9:2
v Zb 8:6
w Mt 28:18 1Ko 15:27 Efe 1:22 Flp 3:21
x Yoh 13:3 Mdo 2:35 1Pe 3:22

Safu ya 2
a Zb 110:1
b Flp 2:7
c Da 7:14
d Isa 53:8 1Pe 1:19 1Yo 4:10 Ufu 5:9
e Isa 53:5 Ro 5:17 1Ti 2:6
f Ro 11:36
g Ro 8:19 2Ko 6:18 1Yo 3:2
h Mdo 5:31 1Ko 8:6 Ebr 12:2
i Lu 24:26 Ebr 5:8
j Yoh 17:19 Ebr 10:14

Ingawa hivyo, sisi bado hatuoni vitu vyote vikiwa vimetiishwa chini yake;[a] **9** lakini tunamwona Yesu, ambaye alikuwa amefanywa kuwa mdogo kidogo kuliko malaika,[b] amevikwa taji la utukufu[c] na heshima kwa kupatwa na kifo,[d] ili kwa fadhili zisizostahiliwa za Mungu aonje kifo kwa ajili ya kila mwanadamu.[e]

10 Kwa maana ilifaa kwa yule ambaye kwa ajili yake vitu vyote vipo[f] na kupitia kwake vitu vyote vipo, katika kuleta wana wengi kwenye utukufu,[g] amfanye Wakili Mkuu[h] wa wokovu wao kuwa mkamilifu kupitia mateso.[i] **11** Kwa maana yeye anayetakasa na wale wanaotakaswa[j] pia wote hutokana na mmoja,[k] na kwa sababu hii yeye haoni aibu kuwaita "ndugu,"[l] **12** kama anavyosema: "Nitalitangaza jina lako kwa ndugu zangu; katikati ya kutaniko nitakusifu wewe kwa wimbo."[m] **13** Na tena: "Tegemeo langu litakuwa katika yeye."[n] Na tena: "Tazama! mimi na watoto wachanga, ambao Yehova alinipa."[o]

14 Basi, kwa kuwa "watoto wachanga" ni washiriki wa damu na mwili, yeye pia vivyo hivyo aliyashiriki mambo hayohayo,[p] ili kupitia kifo[q] chake apate kumwangamiza[r] yule aliye na uwezo wa kusababisha kifo,[s] yaani, Ibilisi;[t] **15** na ili awaweke huru[u] wale wote ambao kwa kuogopa kifo[v] walikuwa wametiishwa chini ya utumwa

k Yoh 1:13; Yoh 20:17; l Mt 12:50; Ro 8:29; m Zb 22:22; Zb 40:9; Lu 4:21; Lu 19:42; n Isa 8:17; o Isa 8:18; Yoh 1:12; 1Yo 3:1; p Mt 11:19; Yoh 1:14; Yoh 11:11; q Isa 53:12; Ro 6:5; Ro 14:9; r Mwa 3:15; Lu 10:18; 1Yo 3:8; s Ayu 1:19; Ayu 2:6; Ufu 6:9; t Yoh 8:44; Yoh 12:31; Ufu 12:9; u Ro 8:21; v Zb 89:48; Isa 25:8; 1Ko 15:26.

katika maisha yao yote.[a]
16 Kwa maana kwa kweli yeye
hawasaidii malaika hata kido-
go, bali anasaidia uzao wa Abra-
hamu.[b] **17** Kwa hiyo alipaswa
kuwa kama "ndugu" zake ka-
tika mambo yote,[c] ili awe ku-
hani mkuu mwenye rehema na
mwaminifu katika mambo yana-
yohusiana na Mungu,[d] kusu-
di atoe dhabihu ya upatanisho[e]
kwa ajili ya dhambi za watu.[f]
18 Kwa kuwa yeye mwenyewe
ameteseka alipokuwa akijari-
biwa,[g] anaweza kuwasaidia wale
wanaojaribiwa.[h]

3 Kwa hiyo, ndugu watakati-
fu, washiriki wa mwito wa
mbinguni,[i] mfikirieni mtume[j]
na kuhani mkuu tunayemki-
ri[k]—Yesu. **2** Alikuwa mwa-
minifu[l] kwa Huyo aliyemfanya
kuwa hivyo, kama Musa[m] ali-
vyokuwa pia katika nyumba
yote ya Huyo.[n] **3** Kwa maa-
na huyu wa mwisho anahesa-
biwa kustahili utukufu[o] kuliko
Musa, kwa kuwa yeye[p] anayeje-
nga nyumba ana heshima kuli-
ko nyumba yenyewe.[q] **4** Bila
shaka, kila nyumba hujengwa
na mtu fulani, lakini yeye aliye-
vijenga vitu vyote ni Mungu.[r]
5 Na Musa akiwa mtumishi[s]
alikuwa mwaminifu katika
nyumba yote yake Huyo kama
ushuhuda wa mambo ambayo
yangesemwa baadaye,[t] **6** la-
kini Kristo alikuwa mwaminifu
akiwa Mwana[u] juu ya nyumba
yake Huyo. Sisi ni nyumba yake
Huyo,[v] ikiwa tunashikilia sana
uhuru wetu wa kusema na kuji-
sifu kwetu juu ya tumaini, ima-
ra mpaka mwisho.[w]

7 Kwa sababu hiyo, kama
vile inavyosema roho[x] takati-
fu: "Leo ikiwa mtaisikiliza sa-
uti yake,[a] **8** msiifanye mioyo
yenu kuwa migumu kama ule
wakati wa kusababisha hasi-
ra kali,[b] kama katika ile siku
ya kufanya jaribu[c] nyikani,[d]
9 ambayo mababu zenu wa-
linijaribu kwa uchunguzi, na
bado walikuwa wameyaona ma-
tendo[e] yangu kwa miaka 40.[f]
10 Kwa sababu hiyo nikachu-
kizwa na kizazi hiki, nikasema,
'Wao hupotea sikuzote katika
mioyo yao,[g] nao wenyewe ha-
wajapata kuzijua njia zangu.'[h]
11 Kwa hiyo niliapa kwa hasi-
ra yangu, 'Hawataingia[i] katika
pumziko langu.'"[j]

12 Jihadharini, akina ndugu,
ili moyo mwovu unaokosa
imani usije ukasitawi ndani ya
yeyote kati yenu kwa kujiondoa
kwa Mungu aliye hai;[k] **13** laki-
ni endeleeni kuhimizana[l] kila
siku, maadamu inaweza kui-
twa "Leo,"[m] ili yeyote kati yenu
asije akafanywa kuwa mgu-
mu kwa nguvu za udanganyi-
fu[n] za dhambi. **14** Kwa maa-
na sisi kwa kweli tunakuwa
washiriki wa Kristo[o] ikiwa tu
tunaushikilia sana uhakika tu-
liokuwa nao mwanzoni imara
mpaka mwisho,[p] **15** huku iki-
semwa: "Leo ikiwa mtaisikili-
za sauti yake,[q] msiifanye mioyo
yenu kuwa migumu kama ule
wakati wa kusababisha hasira
kali."[r]

16 Kwa maana ni nani walio-
sikia na bado wakachochea hasi-
ra kali?[s] Kwa kweli, je, hawaku-
fanya hivyo wale wote waliotoka
Misri chini ya Musa?[t] **17** Zai-
di ya hayo, Mungu alichukizwa
na akina nani kwa miaka 40?[u]

SURA 2

a Isa 25:7
Ro 8:22
b Ga 3:29
Ebr 9:15
Ufu 14:4
c Flp 2:7
d Ebr 5:1
Ebr 7:26
e Ro 3:25
1Yo 2:2
1Yo 4:10
f Ro 5:10
2Ko 5:18
g Mt 26:28
Ebr 4:15
h Ebr 7:25
Ufu 2:10
Ufu 3:10

SURA 3

i Ro 8:30
1Ko 1:9
Flp 3:14
1Th 2:12
2Ti 1:9
2Pe 1:10
j Yoh 3:17
Yoh 7:29
k Ebr 8:1
Ebr 9:15
l Yoh 8:29
Ufu 3:14
m Kum 34:10
n Hes 12:7
o Mt 17:2
2Ko 3:9
p Zek 6:12
Mt 16:18
q 1Ko 3:9
1Pe 2:5
r Mwa 2:3
Efe 3:9
s Kum 3:24
t Kum 18:18
u Mt 17:5
v 2Ko 6:16
Efe 2:19
w Ro 5:2
1Ti 3:13
Ebr 6:11
x 2Sa 23:2
Mdo 1:16

Safu ya 2

a Zb 95:7
b Kut 15:23
c Kut 17:7
d Zb 95:8
e Zb 105:40
f Kut 16:35
Hes 32:13
Kum 8:2
Zb 95:9
g Hes 14:11
Zb 78:8
h Kum 8:3
Zb 95:10
i Hes 14:23
j Zb 95:11
k Ebr 2:1
Ebr 12:15
l 1Th 5:11
m Zb 95:7
n Mk 4:19
2Th 2:10
o Efe 3:6
Ebr 6:4
Ebr 12:8

p Ro 11:22; 2Ko 3:4; 1Yo 3:14; Ufu 2:10; q Zb 95:7; Yoh 6:45; r Zb 95:8; s Kut 17:2; t Hes 14:2; Hes 14:4; u Hes 14:11; Kum 32:21.

Je, haikuwa na wale waliotenda dhambi, ambao mizoga yao
ilianguka nyikani?[a] **18** Lakini aliapa[b] kwa akina nani kwa-
mba hawataingia katika pumziko lake isipokuwa kwa
wale waliotenda kwa kutotii?[c]
19 Kwa hiyo tunaona kwamba
hawakuweza kuingia kwa sababu ya kukosa imani.[d]

4 Kwa hiyo, kwa kuwa aha-
di imebaki ya kuingia kati-
ka pumziko lake,[e] acheni tuo-
gope kwamba wakati fulani ye-
yote kati yenu asije akaonekana
kuwa amepungukiwa.[f] **2** Kwa
maana sisi pia tumetangazi-
wa habari njema,[g] kama wao pia
walivyotangaziwa;[h] lakini neno
lililosikiwa halikuwa na faida
kwao,[i] kwa sababu hawakuu-
nganishwa kwa imani[j] pamo-
ja na wale waliosikia.[k] **3** Kwa
maana sisi ambao tumeonye-
sha imani tunaingia katika pu-
mziko, kama vile ambavyo ame-
sema: "Kwa hiyo niliapa[l] kati-
ka hasira yangu, 'Hawataingia[m]
katika pumziko langu,' "[n] ijapo-
kuwa kazi zake zilimalizwa[o] ta-
ngu kuwekwa msingi wa uli-
mwengu.[p] **4** Kwa maana ka-
tika mahali fulani yeye amese-
ma hivi juu ya siku ya saba:
"Na Mungu akapumzika siku
ya saba kutokana na kazi zake
zote,"[q] **5** na tena katika ma-
hali hapa: "Hawataingia katika
pumziko langu."[r]

6 Basi, kwa kuwa bado ina-
baki watu fulani waingie kati-
ka hilo, na wale ambao wali-
tangaziwa kwanza habari nje-
ma[s] hawakuingia kwa sababu
ya kutotii,[t] **7** yeye tena ana-
weka siku fulani kwa kuse-
ma hivi baada ya wakati mre-
fu sana katika zaburi ya Dau-
di "Leo"; kama ilivyosemwa
hapo juu: "Leo ikiwa mtaisiki-
liza sauti yake,[a] msiifanye mi-
oyo yenu kuwa migumu."[b]
8 Kwa maana kama Yoshua[c]
angekuwa amewaingiza kati-
ka mahali pa pumziko,[d] Mu-
ngu hangesema[e] baadaye juu
ya siku nyingine. **9** Kwa hiyo
bado limebaki pumziko la saba-
to kwa ajili ya watu wa Mungu.[f]
10 Kwa maana mtu ambaye
ameingia katika pumziko[g] la
Mungu yeye mwenyewe pia
amepumzika kutokana na kazi
zake mwenyewe,[h] kama Mungu
alivyopumzika kutokana na
kazi zake mwenyewe.

11 Kwa hiyo acheni sisi tufa-
nye yote tunayoweza ili kuingia
katika pumziko hilo, yeyote asi-
je akaanguka katika kielelezo
kilekile cha kutotii.[i] **12** Kwa
maana neno[j] la Mungu liko hai[k]
nalo lina nguvu[l] na ni lenye ma-
kali zaidi kuliko upanga wowo-
te wenye makali kuwili[m] nalo
huchoma hata kufikia kugawa-
nya nafsi[n] na roho,[o] na viungo
na urojorojo wake, nalo linaweza
kutambua fikira na makusudio
ya moyo.[p] **13** Na hakuna kiu-
mbe kisichokuwa wazi macho-
ni pake,[q] bali vitu vyote viko
uchi navyo vimefunuliwa wazi
machoni pake yeye ambaye tu-
natoa hesabu kwake.[r]

14 Basi, kwa kuwa tuna ku-
hani mkuu sana ambaye ame-
pita katika mbingu,[s] Yesu Mwa-
na wa Mungu,[t] acheni tuendelee
kumkiri yeye.[u] **15** Kwa ma-
ana tuna kuhani mkuu, si mtu
ambaye hawezi kuusikitikia[v]

SURA 3

a Hes 14:22
Hes 14:29
1Ko 10:5
1Ko 10:10
Yud 5
b Kum 1:34
Zb 106:26
c Hes 14:30
Kum 1:35
d Ebr 4:6

SURA 4

e Mwa 2:3
Kut 20:11
Ebr 3:11
f Ga 5:4
Ebr 3:12
Ebr 12:15
g Mt 4:23
Mdo 15:7
Kol 1:23
h Kut 19:5
Kum 32:1
Mdo 10:36
i Kum 32:15
j Kum 32:20
k Isa 10:22
l Kum 1:34
m Hes 14:23
Kum 1:35
n Zb 95:11
Ebr 3:11
o Kut 31:17
p Yoh 17:24
Efe 1:4
q Mwa 2:2
r Zb 95:11
s Kum 32:1
t Hes 14:30
Kum 31:27

Safu ya 2

a Zb 95:7
b Zb 95:8
c Kut 24:13
Kum 1:38
Kum 31:7
d Yos 22:4
e Yer 6:16
f Isa 66:23
Zek 14:16
Mk 2:28
g Mwa 2:2
h Ufu 14:13
i Zb 95:11
Ro 11:30
Ebr 3:17
j Mt 15:6
Mdo 11:1
1Th 2:13
1Th 4:15
k Yer 23:29
Zek 4:6
Yoh 2:17
1Pe 1:23
l 2Ko 10:4
m Isa 49:2
Efe 6:17
n Mt 16:26
o Mdo 17:16
Ro 1:9
Kol 2:5
p Met 21:2
Met 24:12
Yoh 12:48
1Ko 4:5

q Zb 7:9; Zb 90:8; Met 15:11; r Ayu 31:14; Mdo 17:31; Ro 2:16; Ro 14:12; s Ebr 7:26; t Mt 26:63; Mk 1:11; Ebr 1:2; u Ebr 3:1; Ebr 10:23; v Isa 53:4; Isa 61:1; Ebr 2:17.

udhaifu wetu, bali yeye ambaye
amejaribiwa katika mambo yote
kama sisi wenyewe, lakini bila
kuwa na dhambi.[a] **16** Basi na
tukikaribie,[b] tukiwa na uhuru
wa kusema,[c] kiti cha ufalme cha
fadhili zisizostahiliwa, ili tupo-
kee rehema na kupata fadhili zi-
sizostahiliwa kuwa msaada kwa
wakati unaofaa.[d]

5 Kwa maana kila kuhani
mkuu anayechukuliwa ku-
toka kati ya wanadamu huwe-
kwa rasmi kwa ajili ya wanada-
mu juu ya mambo yanayohusi-
ana na Mungu,[e] ili atoe zawadi
na dhabihu kwa ajili ya dha-
mbi.[f] **2** Yeye anaweza kuwa-
tendea kwa kiasi wale wasiojua
na wanaokosea kwa kuwa yeye
pia amezungukwa na udhaifu
wake mwenyewe,[g] **3** na kwa
sababu ya huo ana wajibu wa
kutoa matoleo ya dhambi kwa
ajili yake mwenyewe kama vile
kwa ajili ya watu.[h]

4 Pia, mtu huchukua heshi-
ma hii, si kwa kupenda kwake
mwenyewe,[i] bali tu Mungu ana-
pomwita,[j] kama Haruni[k] pia ali-
vyoitwa. **5** Vivyo hivyo pia
Kristo hakujitukuza mwenye-
we[l] kwa kuwa kuhani mkuu,[m]
bali alitukuzwa[n] na yeye aliye-
sema hivi kumhusu: "Wewe ni
mwanangu; mimi, leo, nimeku-
wa baba yako."[o] **6** Kama vile
anavyosema pia mahali pengi-
ne: "Wewe ni kuhani milele
kwa mfano wa Melkizedeki."[p]

7 Katika siku za mwili wake
wenye nyama Kristo alitoa dua
na pia maombi[q] kwa Yule aliye-
kuwa na uwezo wa kumwokoa
kutoka katika kifo, pamoja na
vilio vyenye nguvu[r] na macho-
zi, naye akasikiwa vizuri kwa
sababu ya kumwogopa[a] Mu-
ngu. **8** Ijapokuwa yeye aliku-
wa Mwana, alijifunza kutii ku-
tokana na mambo aliyoteseka;[b]
9 na baada ya yeye kufanywa
kuwa mkamilifu[c] akawa ndiye
mwenye daraka la wokovu[d] wa
milele kwa wale wote wanao-
mtii,[e] **10** kwa sababu Mungu
amemwita jina, kuhani mkuu
kwa mfano wa Melkizedeki.[f]

11 Kumhusu yeye sisi tuna
mengi ya kusema na yaliyo ma-
gumu kufafanuliwa, kwa kuwa
mmekuwa wazito katika kusi-
kia kwenu.[g] **12** Kwa maana,
kwa kweli, ijapokuwa mnapa-
swa kuwa walimu[h] kwa saba-
bu ya wakati, ninyi mnahita-
ji tena mtu awafundishe tangu
mwanzo mambo ya msingi[i] ya
maneno matakatifu ya Mungu;[j]
nanyi mmekuwa kama wana-
ohitaji maziwa, si chakula ki-
gumu.[k] **13** Kwa maana kila
mtu anayetumia maziwa hafa-
hamu neno la uadilifu, kwa
maana yeye ni mtoto mchanga.[l]
14 Lakini chakula kigumu ni
cha watu wakomavu, cha wale
ambao kwa kutumia, nguvu
zao za ufahamu[m] zimezoezwa
kutofautisha yaliyo sawa na ya-
liyo makosa pia.[n]

6 Kwa sababu hiyo, kwa
kuwa sasa tumeliacha fu-
ndisho la msingi[o] juu ya Kri-
sto,[p] na tusonge mbele kuele-
kea ukomavu,[q] tusiweke msingi
tena,[r] yaani, kutubu matendo
yaliyokufa,[s] na imani kwa Mu-
ngu,[t] **2** fundisho juu ya ma-
batizo[u] na kuwekewa mikono,[v]
kufufuliwa kwa wafu[w] na hu-
kumu[x] ya milele. **3** Na hili tu-

SURA 4
a 2Ko 5:21; Ebr 7:26; 1Pe 2:22
b Efe 2:18; Ebr 10:19
c Efe 3:12
d Ebr 13:6

SURA 5
e Kut 40:13
f Law 5:6; Ebr 8:3
g Ebr 2:18; Ebr 4:15
h Law 9:7; Law 16:6; Mal 2:7
i 2Nya 26:18
j Yoh 3:27
k Kut 28:1
l Yoh 8:54
m Ebr 4:14
n Yoh 12:28
o Zb 2:7; Mdo 13:33
p Zb 110:4; Ebr 7:17
q Lu 22:44
r Mt 26:39; Yoh 12:27

Safu ya 2
a Lu 12:5
b Mt 26:39; Yoh 10:17; Flp 2:8
c Law 8:33; Ebr 7:28
d Isa 45:17; Isa 49:6; Isa 53:11; Lu 1:69
e Yoh 3:16
f Zb 110:4
g 2Pe 3:16
h Efe 4:11
i Ebr 6:1
j Mdo 7:38; Ro 3:2; 1Pe 4:11
k 1Ko 3:2
l 1Ko 13:11; Efe 4:14
m Mk 7:18; Efe 1:18
n Isa 7:15; Ro 16:19; Flp 1:10; 1Th 5:21

SURA 6
o 1Ko 3:1; Ebr 5:12
p Kol 1:27; 1Ti 3:16
q 1Ko 13:11; 1Ko 14:20; Efe 4:13; Flp 3:16; Ebr 5:14
r 1Ko 3:10
s Efe 4:22
t 1Th 1:8
u Mdo 19:4; Ro 6:3
v Mdo 6:6; 1Ti 5:22
w Mt 22:31; Yoh 5:29; Yoh 11:25;
x Mdo 17:31; 2Pe 3:7; Ufu 20:12.

talifanya, ikiwa kwa kweli Mungu ataruhusu.[a]

4 Kwa maana haiwezekani kamwe kwa habari ya wale
ambao wametiwa nuru[b] mara
moja kwa wakati wote, na ambao
wameonja zawadi ya bure[c] ya
kimbingu, na ambao wamekuwa washiriki wa roho takatifu,[d]
5 na ambao wameonja[e] neno
zuri la Mungu na nguvu za mfumo wa mambo unaokuja,[f] **6** lakini ambao wameanguka,[g] kuwarudisha tena kwenye toba,[h]
kwa sababu wanamtundika upya
mtini Mwana wa Mungu kwa ajili yao wenyewe na kumfunua
yeye kwenye aibu ya hadharani.[i]
7 Kwa mfano, udongo unaokunywa mvua ambayo huja mara
nyingi juu yake, na kisha unazaa
mimea inayofaa kwa wale ambao
huo hulimwa kwa ajili yao,[j] hupokea malipo ya baraka kutoka kwa Mungu. **8** Lakini ukizaa miiba na mibaruti, hukataliwa na huwa karibu kulaaniwa;[k]
nao mwisho wake huchomwa.[l]

9 Hata hivyo, kwa hali yenu,
wapendwa, tunasadiki juu ya
mambo yaliyo bora na mambo
yanayofuatana na wokovu, ijapokuwa tunasema jinsi hii.
10 Kwa maana Mungu hakosi
kuwa mwadilifu hivi kwamba
asahau kazi yenu na upendo
mlioonyesha kwa ajili ya jina
lake,[m] kwa kuwa mmewahudumia watakatifu[n] nanyi mna-
endelea kuhudumu. **11** Lakini
tunatamani kila mmoja
wenu aonyeshe bidii ileile ili
kuwa na uhakikisho kamili[o]
wa tumaini[p] mpaka mwisho,[q]
12 ili msiwe goigoi,[r] bali muwe
waigaji[s] wa wale ambao kupitia imani na subira huzirithi
ahadi.[t]

SURA 6

a Yak 4:15
b Efe 1:18
Ebr 10:26
c Mdo 10:45
Efe 3:7
Yak 1:17
d Mdo 15:8
Ga 3:5
Ebr 2:4
e 1Pe 2:3
f 2Ko 5:5
Efe 1:14
g Zb 119:118
2Ko 11:13
Ebr 10:39
1Yo 2:19
h Mt 12:32
i Ebr 10:29
j Mwa 1:11
k Mwa 3:18
l Mt 13:30
m 1Th 1:3
Ebr 10:32
n Ro 15:25
2Ko 8:4
2Ti 1:18
o Kol 2:2
p 1Pe 1:3
q Ebr 3:14
r Ro 12:11
Ufu 2:4
s 1Ko 11:1
t Ebr 10:36
Yak 5:10

Safu ya 2

a Ro 4:20
b Mwa 22:16
Zb 105:9
Isa 45:23
Lu 1:73
c Mwa 22:17
d Ebr 11:17
e Kut 22:11
Yer 12:16
f Mwa 31:53
Mwa 47:31
g Ga 3:29
h Mal 3:6
i Hes 23:19
1Sa 15:29
Tit 1:2
j Ro 5:4
Kol 1:5
k 1Pe 1:3
l Law 16:2
Law 16:12
Yoh 14:3
Ebr 9:7
Ebr 10:20
m Ebr 4:14
n Zb 110:4
Ebr 5:6

SURA 7

o Mwa 14:18
p Mwa 14:19
q Mwa 14:20

13 Kwa maana Mungu alipoitoa ahadi yake kwa Abrahamu,[a]
kwa kuwa hangeweza kuapa
kwa yeyote aliye mkubwa zaidi,
aliapa[b] kwa nafsi yake mwenyewe, **14** akisema: "Hakika nitakubariki, nami nitakuzidisha."[c]
15 Na hivyo baada ya Abrahamu kuonyesha subira, aliipata ahadi hiyo.[d] **16** Kwa maana watu huapa kwa aliye mkubwa zaidi,[e] na kiapo chao ndicho mwisho wa kila bishano,
kwa kuwa hicho ni uhakikisho wa kisheria kwao.[f] **17** Vivyo hivyo Mungu, alipokusudia kuwaonyesha kwa wingi zaidi warithi[g] wa ile ahadi
kule kutobadilika[h] kwa shauri lake, aliingilia kati kwa kiapo, **18** ili, kupitia mambo mawili yasiyobadilika ambayo katika hayo Mungu hawezi kamwe
kusema uwongo,[i] sisi ambao tumekimbia kwenda katika kimbilio tupate kuwa na kitia-moyo
chenye nguvu kushikilia tumaini[j] lililowekwa mbele yetu.
19 Tumaini[k] hilo tunalo kama
nanga ya nafsi, likiwa hakika na imara, nalo huingia mle
ndani ya pazia,[l] **20** ambamo
mtangulizi ameingia kwa ajili
yetu,[m] Yesu, ambaye amekuwa kuhani mkuu milele kwa
mfano wa Melkizedeki.[n]

7 Kwa maana Melkizedeki
huyu, mfalme wa Salemu,
kuhani wa Mungu Aliye Juu
Zaidi,[o] aliyekutana na Abraham akirudi kutoka kuwamaliza wafalme kisha akambariki[p]
2 na ambaye Abrahamu alimgawia sehemu ya kumi katika vitu vyote,[q] kwanza kabisa, kwa tafsiri, yeye ni "Mfalme wa Uadilifu," na kisha pia ni

mfalme wa Salemu,[a] yaani,
"Mfalme wa Amani." **3** Kwa
kuwa asiye na baba, asiye na
mama, bila ukoo, akiwa hana
mwanzo wa siku[b] wala mwi-
sho wa uzima, bali akiwa ame-
fanywa kama Mwana wa Mu-
ngu,[c] anadumu akiwa kuhani
daima.[d]

4 Oneni, basi, jinsi alivyo-
kuwa mkuu mtu huyu
ambaye Abrahamu, yule ki-
chwa cha familia, alimtolea se-
hemu ya kumi kutokana na zile
nyara kuu.[e] **5** Ni kweli, watu
kutoka katika wana wa Lawi[f]
ambao hupokea cheo chao cha
ukuhani wana amri ya kuku-
sanya sehemu za kumi[g] kutoka
kwa watu[h] kulingana na She-
ria, yaani, kutoka kwa ndu-
gu zao, hata kama hao wame-
toka katika viuno vya Abra-
hamu;[i] **6** lakini mtu ambaye
ukoo[j] wake haukutokana nao
alichukua sehemu za kumi ku-
toka kwa Abrahamu[k] na ku-
mbariki yeye ambaye alikuwa
na zile ahadi.[l] **7** Basi bila ma-
bishano, mdogo hubarikiwa na
mkubwa.[m] **8** Na katika hali
ile moja watu wanaokufa ndio
hupokea sehemu za kumi,[n] la-
kini katika hali ile nyingine
ni mtu ambaye imeshuhudiwa
kwamba anaishi.[o] **9** Na, niki-
tumia neno hili, kupitia Abra-
hamu hata Lawi ambaye hupo-
kea sehemu za kumi amelipa
sehemu za kumi, **10** kwa ma-
ana alikuwa bado katika viuno[p]
vya babu yake wakati Melkize-
deki alipokutana naye.[q]

11 Basi, kama kwa kweli
ukamilifu[r] ungekuwa ni kupi-
tia ukuhani wa Walawi,[s] (kwa
maana huo ukiwa sehemu kuu
watu walipewa Sheria,)[t] ku-
ngekuwa na uhitaji gani zaidi[a]
wa kuhani mwingine kusima-
ma kwa mfano wa Melkizedeki[b]
na asisemwe kuwa kwa mfano
wa Haruni? **12** Maana kwa
kuwa ukuhani unabadilishwa,[c]
basi kunakuja kuwa na uhi-
taji wa kubadilishwa kwa she-
ria[d] pia. **13** Kwa maana yule
mtu ambaye mambo haya ya-
nasemwa kumhusu amekuwa
ni mshiriki wa kabila[e] lingi-
ne, ambalo kutoka kwake ha-
kuna yeyote ambaye ametumi-
kia rasmi kwenye madhabahu.[f]
14 Kwa maana ni wazi kabi-
sa kwamba Bwana wetu ame-
tokana na Yuda,[g] kabila ambalo
Musa hakusema lolote juu yake
kuhusiana na makuhani.

15 Na bado ni wazi zaidi kwa-
mba kwa mfano wa Melkizedeki[h]
anasimama kuhani[i] mwingine,
16 ambaye amekuwa hivyo, si
kulingana na sheria ya amri ina-
yotegemea mwili,[j] bali kuliinga-
na na nguvu za uzima usiowe-
za kuharibika,[k] **17** kwa maa-
na katika kutoa ushahidi ime-
semwa: "Wewe ni kuhani milele
kwa mfano wa Melkizedeki."[l]

18 Hakika, basi, ile amri iliyo-
tangulia inawekwa kando kwa
sababu ya udhaifu[m] wake na ku-
tofaa[n] kwake. **19** Kwa maa-
na Sheria haikufanya kitu cho-
chote kuwa kikamilifu,[o] lakini
kuingizwa kwa tumaini[p] bora
kulifanya mambo yawe maka-
milifu, ambalo kupitia hilo tu-
namkaribia Mungu.[q] **20** Pia,
kwa kadiri ambayo haikuwa bila
kiapo rasmi, **21** (kwa maana
kwa kweli kuna watu ambao
wamekuwa makuhani bila ki-
apo rasmi, lakini kuna mmo-
ja mwenye kiapo rasmi kupitia
Yule aliyesema hivi kumhusu:

SURA 7

a Mwa 14:18
Zb 76:2
b Met 8:23
c Mt 16:16
d Zb 110:4
e Mwa 14:20
f Kut 40:15
Hes 18:21
g Hes 18:26
Kum 14:28
h Law 7:34
i Yoh 8:33
j Ezr 2:62
k Mwa 14:20
l Mwa 12:7
Mwa 17:6
Mwa 22:17
Ro 4:13
Ga 3:16
m Ebr 11:20
n Hes 18:21
o Ebr 7:3
p Kut 1:5
Ro 7:9
q Mwa 14:18
r Ro 3:20
Ga 2:21
Ebr 7:19
Ebr 9:9
s Ebr 10:1
t Ga 3:19

Safu ya 2

a Yer 31:31
Ebr 8:7
b Zb 110:4
c Ebr 8:1
d Ro 3:27
1Ko 9:21
Ga 6:2
Kol 2:14
e Ufu 5:5
f Hes 18:7
2Nya 26:18
g Mwa 49:10
Isa 11:1
Mt 1:3
Lu 3:33
h Zb 110:4
i Ebr 3:1
Ebr 7:26
j Ro 7:14
k Ro 6:9
1Ti 6:16
Ufu 1:18
l Zb 110:4
Ebr 5:6
Ebr 6:20
m Ro 8:3
Ga 4:9
n Ebr 9:9
Ebr 13:9
o Mdo 13:39
Ga 2:16
Ebr 10:1
p 1Ti 1:1
Ebr 6:18
1Pe 1:3
q Yoh 14:6
Ro 5:2
Ebr 4:16

"Yehova ameapa[a] (naye hatajuta), 'Wewe ni kuhani milele,'")[b] **22** kwa kadiri hiyo pia
Yesu amekuwa yule aliyetolewa kuwa rehani ya agano
bora.[c] **23** Zaidi ya hayo, ilikuwa lazima wengi wawe maku-
hani kwa mfuatano[d] kwa sababu ya kuzuiwa na kifo[e] wasie-
ndelee kuwa hivyo, **24** lakini yeye kwa sababu ya kuendelea
kuwa hai milele[f] ana ukuhani wake bila kuwa na waandami-
zi wowote. **25** Kwa hiyo yeye anaweza pia kuwaokoa kwa
ukamili wale wanaomkaribia Mungu kupitia yeye, kwa saba-
bu yeye yuko hai sikuzote ili kuwaombea.[g]

26 Kwa maana kuhani mkuu wa namna hiyo alitufaa sisi,[h]
mshikamanifu,[i] asiye na hila,[j] asiye na unajisi,[k] aliyetengwa
kutoka kwa watenda-dhambi,[l] na kuwa juu zaidi kuliko mbi-
ngu.[m] **27** Yeye hahitaji kila siku,[n] kama wale makuhani
wakuu wanavyofanya, kutoa dhabihu, kwanza kwa ajili
ya dhambi zake mwenyewe[o] kisha kwa ajili ya zile za watu:[p]
(kwa maana yeye alifanya hilo mara moja[q] kwa wakati wote ali-
pojitoa[r] mwenyewe;) **28** kwa maana Sheria huweka rasmi
kuwa makuhani wakuu[s] watu walio na udhaifu,[t] lakini neno la
kiapo[u] rasmi lililokuja baada ya Sheria humweka rasmi Mwana,
ambaye amekamilishwa[v] milele.

8 Basi kuhusu mambo yana-
yozungumzwa jambo kuu
ni hili: Sisi tuna kuhani mkuu[w]
wa namna hii, naye ameketi
kwenye mkono wa kuume wa
kiti cha ufalme cha Ukuu mbi-
nguni,[x] **2** mtumishi wa watu

SURA 7

a Ebr 6:18
b Zb 110:4
c Yer 31:31
Mt 26:28
1Ko 11:25
Ebr 8:6
Ebr 9:15
Ebr 12:24
d 1Nya 6:4
e Hes 20:28
Yos 24:33
f Lu 1:33
Ebr 7:16
Ebr 13:8
g Ro 8:34
1Ti 2:5
Ebr 9:24
1Yo 2:1
h Ebr 4:15
i Isa 16:5
Ebr 3:2
j Zek 9:9
k Isa 53:9
1Pe 2:22
l Yoh 8:46
m Efe 1:20
Ebr 4:14
1Pe 3:22
n Hes 28:3
o Law 9:8
p Law 9:15
q Ro 6:10
r Ebr 9:28
Ebr 10:14
s Kut 29:9
t Law 16:11
u Zb 2:7
Zb 110:4
v Ebr 2:10
Ebr 5:9

SURA 8

w Zek 6:13
Ebr 3:1
Ebr 7:26
x Zb 110:1
Ebr 1:3

Safu ya 2

a Ebr 9:8
Ebr 9:24
b Kut 25:9
Zb 84:1
Ebr 3:4
c Ebr 9:11
d Ebr 5:1
e Yoh 6:51
Efe 5:2
f Ebr 7:14
g Ebr 9:9
Ebr 9:24
h Kol 2:17
Ebr 10:1
i Ebr 9:9
j Kut 25:9
k Kut 25:40
Kut 26:30
Hes 8:4
Mdo 7:44
l 1Ti 2:5
Ebr 12:24
m 1Ko 11:25
Ebr 7:22
Ebr 9:15

wote wa mahali patakatifu[a] na
wa hema la kweli, ambalo Ye-
hova[b] alisimamisha, na si mwa-
nadamu.[c] **3** Kwa maana kila
kuhani mkuu huwekwa rasmi
ili kutoa zawadi na dhabihu;[d]
kwa hiyo ilikuwa lazima pia
kwa huyu kuwa na kitu fula-
ni cha kutoa.[e] **4** Sasa, kama
angekuwa duniani, hangeku-
wa kuhani,[f] kukiwa na watu
ambao hutoa zawadi kulinga-
na na Sheria, **5** lakini watu
ambao wanatoa utumishi mta-
katifu katika mfano wa uhali-
si[g] na kivuli[h] cha vitu vya mbi-
nguni; kama vile Musa, alipo-
kuwa karibu kumaliza hema,[i]
alipewa amri ya kimungu:[j]
Kwa maana yeye anasema:
"Uhakikishe kwamba umevifa-
nya vitu vyote kulingana na
mfano wake ambao wewe ulio-
nyeshwa mlimani."[k] **6** Lakini
sasa Yesu amepata utumishi wa
watu wote ulio bora zaidi, hivi
kwamba yeye pia ni mpatani-
shi[l] wa agano lililo bora kwa
kulinganishwa,[m] ambalo lime-
fanywa imara kisheria juu ya
ahadi zilizo bora.[n]

7 Kwa maana ikiwa agano
lile la kwanza lingekuwa bila
kosa, mahali hapangetafutwa
kwa ajili ya la pili;[o] **8** kwa
maana yeye anawalaumu wale
watu anaposema: "'Tazama!
Siku zinakuja,' asema Yehova,
'nami nitafanya agano jipya pa-
moja na nyumba ya Israeli na
nyumba ya Yuda;[p] **9** si kuli-
ngana na lile agano[q] ambalo
nilifanya pamoja na mababu
zao katika ile siku nilipowashi-
ka mkono na kuwatoa katika
nchi ya Misri,[r] kwa sababu

n Zb 110:4; Ro 8:17; o Ebr 7:11; Ebr 7:18; p Yer 31:31; q Kum 4:23; r Kut 12:51.

hawakuendelea kulishika agano
langu,[a] hivi kwamba nikaacha
kuwajali,' asema Yehova."[b]
10 "'Kwa maana hili ndilo
agano nitakalofanya pamoja
na nyumba ya Israeli baada ya
siku hizo,' asema Yehova. 'Ni-
tazitia sheria zangu katika aki-
li yao, nami nitaziandika ka-
tika mioyo yao.[c] Nami nitaku-
wa Mungu wao,[d] nao watakuwa
watu wangu.[e]
11 "'Nao hawatafundishana
kwa vyovyote kila mtu na raia
mwenzake wala kila mtu na
ndugu yake, wakisema: "Mjue
Yehova!"[f] Kwa maana wote wa-
tanijua mimi,[g] kuanzia yule
aliye mdogo zaidi mpaka yule
aliye mkubwa zaidi kati yao.
12 Kwa maana nitaonyesha re-
hema kwa matendo yao yasi-
yo ya uadilifu, nami sitaziku-
mbuka[h] tena dhambi[i] zao hata
kidogo.'"
13 Kwa kusema "agano ji-
pya," Yeye amelifanya lile la za-
mani kuchakaa.[j] Basi kile kina-
chofanywa kuchakaa na kuze-
eka kiko karibu kutoweka.[k]

9 Basi, kwa upande wake, lile
agano la zamani lilikuwa
na maagizo ya utumishi mtaka-
tifu[l] na mahali pake patakatifu
pa kidunia.[m] **2** Kwa maana
kilijengwa chumba cha hema
cha kwanza[n] ambacho ndani
yake mlikuwa kile kinara cha
taa[o] na pia meza[p] na wonyesho
wa mikate;[q] nacho kinaitwa
"Mahali Patakatifu."[r] **3** Laki-
ni nyuma ya pazia[s] la pili kuli-
kuwa na chumba cha hema ki-
lichoitwa "Patakatifu Zaidi."[t]
4 Hicho kilikuwa na chetezo[u]
cha dhahabu na sanduku la
agano[v] likiwa limefunikwa ku-
zunguka pande zote kwa dha-
habu,[a] ambalo ndani yake mli-
kuwa na mtungi wa dhahabu
wenye mana[b] na ile fimbo ya
Haruni iliyochipuka[c] na yale
mabamba[d] ya agano; **5** lakini
upande wake wa juu palikuwa
na wale makerubi[e] wenye utu-
kufu waliokifunika kile kifuni-
ko cha upatanisho.[f] Lakini sasa
si wakati wa kusema kirefu ha-
bari za vitu hivyo.
6 Baada ya vitu hivyo kuje-
ngwa kwa njia hiyo, makuha-
ni huingia katika chumba cha
kwanza cha hema[g] nyakati zote
ili kutoa utumishi mtakatifu;[h]
7 lakini ndani ya chumba cha
pili kuhani mkuu peke yake
huingia mara moja kwa mwa-
ka,[i] wala si bila damu,[j] amba-
yo yeye huitoa kwa ajili yake
mwenyewe[k] na kwa ajili ya dha-
mbi za hali ya watu[l] ya kutojua.
8 Hivyo roho takatifu hufa-
nya iwe wazi kwamba njia[m] ya
kuingia ndani ya mahali pa-
takatifu ilikuwa bado haijafu-
nuliwa wakati lile hema la za-
mani lilipokuwa limesimama.[n]
9 Hema hili ni mfano[o] kwa aji-
li ya wakati uliowekwa ambao
upo sasa,[p] na kwa kupatana
nalo zawadi na dhabihu pia zi-
natolewa.[q] Hata hivyo, hizo ha-
ziwezi kumfanya mtu anaye-
toa utumishi mtakatifu awe
mkamilifu[r] kuhusiana na dha-
miri[s] yake, **10** bali zinahusu
tu vyakula[t] na vinywaji[u] na
mabatizo[v] mbalimbali. Hayo
yalikuwa matakwa ya kishe-
ria yanayohusiana na mwili[w]
nayo yaliamriwa mpaka wakati
uliowekwa wa kunyoosha ma-
mbo.[x]
11 Hata hivyo, Kristo alipo-
kuja akiwa kuhani mkuu[y] wa
mambo mema ambayo yame-

SURA 8
a Kum 32:15
b Yer 31:32
c Eze 11:19
Ro 2:29
d 2Ko 6:16
e Yer 31:33
Zek 8:8
Ebr 10:16
f Ho 2:20
g Isa 54:13
Yoh 6:45
h Yer 31:34
Ebr 10:17
i Zb 103:12
Ro 11:27
j Ro 10:4
Ebr 7:12
k Mt 23:38
Efe 2:14
Kol 2:14

SURA 9
l Law 4:6
Ebr 9:9
m Kut 25:8
n Kut 26:33
o Kut 40:24
Hes 4:9
p Kut 40:22
q Kut 40:23
r Kut 26:33
s Kut 36:35
t Kut 26:34
u Law 16:12
Ufu 8:3
v Kut 40:21

Safu ya 2
a Kut 25:11
b Kut 16:33
c Hes 17:10
d Kut 32:15
2Nya 5:10
e Kut 25:22
Hes 7:89
f Kut 25:18
1Nya 28:11
g Law 24:3
h Law 24:4
i Law 16:2
Ebr 9:25
j Kut 30:10
Law 16:14
k Law 16:6
l Law 16:15
m Yoh 14:6
n Ebr 10:20
o Ebr 8:5
p Kol 2:17
Ebr 10:1
q Law 23:38
r Ga 3:21
Ebr 7:11
Ebr 7:19
Ebr 8:6
s 1Pe 3:21
t Law 11:2
u Law 10:9
Law 11:34
v Law 11:40
w Hes 19:13
x Isa 2:4
Yoh 1:17
Ebr 1:2
y Ebr 4:14

kwisha kuwa, kupitia hema ku-
bwa zaidi na kamilifu zaidi
ambalo halikufanywa kwa mi-
kono, yaani, si la uumbaji huu,[a]
12 aliingia, si kwa damu ya
mbuzi na ya ng'ombe-dume wa-
changa,[b] bali kwa damu yake
mwenyewe,[c] mara moja kwa
wakati wote ndani ya mahali
patakatifu na kupata ukombo-
zi wa milele kwa ajili yetu.[d]
13 Kwa maana ikiwa damu ya
mbuzi[e] na ya ng'ombe-dume[f] na
majivu[g] ya ndama-jike yaliyo-
nyunyizwa juu ya wale ambao
wametiwa unajisi[h] hutakasa
kufikia usafi wa mwili,[i] **14** je,
si zaidi damu[j] ya Kristo, amba-
ye kupitia roho inayodumu mi-
lele alijitoa[k] mwenyewe bila do-
sari kwa Mungu, itazisafisha[l]
dhamiri zetu kutoka katika
matendo yaliyokufa[m] ili tutoe
utumishi mtakatifu[n] kwa Mu-
ngu aliye hai?

15 Basi ndiyo sababu yeye ni
mpatanishi[o] wa agano jipya, ili,
kwa sababu kifo kimetokea kwa
ajili ya wao kuachiliwa huru
kwa fidia[p] kutoka kwenye ma-
kosa chini ya lile agano la za-
mani,[q] wale ambao wameitwa
waipokee ahadi ya urithi unao-
dumu milele.[r] **16** Kwa maana
mahali palipo na agano,[s] kifo
cha yule mwanadamu mwenye
kufanya agano kinahitaji kua-
ndaliwa. **17** Kwa maana aga-
no ni halali juu ya watu wafu,
kwa kuwa halitendi wakati yule
mwanadamu mwenye kufanya
agano akiwa hai. **18** Kwa hiyo
lile agano la zamani[t] halikuzi-
nduliwa bila damu.[u] **19** Kwa
maana wakati kila amri ku-
lingana na Sheria ilipokuwa
imesemwa na Musa kwa watu
wote,[v] alichukua damu ya wale

SURA 9

a Ebr 9:24
b Mt 20:28
1Ti 2:6
Ebr 12:24
Ebr 13:20
c Ebr 8:3
d Isa 45:17
Da 9:24
Ro 11:27
Ebr 10:17
e Law 16:15
f Law 16:6
g Hes 19:9
h Hes 19:17
i Hes 19:19
j Law 17:11
1Pe 1:19
k Efe 5:2
l Ebr 10:2
1Yo 1:7
m 1Ko 6:11
Ebr 6:1
n Ro 12:1
Flp 3:3
Ebr 12:28
o 1Ti 2:5
Ebr 12:24
p Mt 20:28
Lu 22:20
q Ga 3:13
r Ro 8:17
s Mwa 21:27
Ga 3:15
t Kut 24:7
u Kut 24:6
v Kut 24:3

Safu ya 2

a Hes 19:6
b Kut 24:8
c Law 16:16
d Kut 29:12
Law 8:15
Law 16:18
e Law 17:11
f Law 9:9
g Efe 1:7
h Ebr 8:5
Ebr 9:9
i Law 16:19
Law 16:20
j Ebr 8:2
k Kol 2:17
l Ebr 6:20
Ebr 9:12
Ebr 10:19
m Law 16:15
Yoh 16:28
Ro 8:34
n Law 16:2
o Law 16:34
p Efe 1:4
q Ga 4:4
1Pe 1:20
r Ebr 7:27
1Pe 3:18
s Mt 24:3
1Ko 10:11
Ebr 1:2
t Isa 53:12
Da 9:24
1Ko 5:7
u Kut 29:9
Law 16:11
Ebr 7:27
Ebr 7:28
Ebr 9:7
v Yoh 17:1
w Ro 6:10

ng'ombe-dume wachanga na
ya wale mbuzi pamoja na maji
na sufu nyekundu na hisopo[a]
na kukinyunyizia kile kitabu na
watu wote, **20** akisema: "Hii
ndiyo damu ya agano ambalo
Mungu ameweka kuwa amri juu
yenu."[b] **21** Naye alilinyunyi-
zia lile hema[c] na vyombo vyote
vya utumishi wa watu wote vi-
vyo hivyo kwa damu.[d] **22** Ndi-
yo, karibu vitu vyote husafishwa
kwa damu[e] kulingana na Sheria,
na damu isipomwagwa[f] hakuna
msamaha unaotokea.[g]

23 Kwa hiyo ilikuwa lazi-
ma kwamba mifano[h] ya uhalisi
wa vitu vilivyo mbinguni isafi-
shwe kwa njia hizo,[i] lakini vitu
vya mbinguni vyenyewe visafi-
shwe kwa dhabihu zilizo bora
kuliko dhabihu za namna hiyo.
24 Kwa maana Kristo hakui-
ngia mahali patakatifu palipofa-
nywa kwa mikono,[j] ambapo ni
mfano wa uhalisi,[k] bali aliingia
mbinguni kwenyewe,[l] ili sasa ao-
nekane mbele za uso wa Mu-
ngu kwa ajili yetu.[m] **25** Wala
si ili ajitoe mwenyewe mara nyi-
ngi, kama vile kuhani mkuu
anavyoingia mahali patakatifu[n]
mwaka baada ya mwaka[o] akiwa
na damu isiyo yake mwenyewe.
26 Kama sivyo, ingekuwa lazi-
ma ateseke mara nyingi tangu
kuwekwa msingi[p] wa ulimwe-
ngu. Lakini sasa amejifunua[q]
mara moja[r] kwa wakati wote
kwenye umalizio wa mifumo
ya mambo[s] ili kuondolea mba-
li dhambi kupitia dhabihu yake
mwenyewe.[t] **27** Na kama vile
watu wamewekewa akiba[u] kufa
mara moja kwa wakati wote,
lakini baada ya hilo ni huku-
mu,[v] **28** vivyo hivyo pia Kri-
sto alitolewa[w] mara moja kwa

wakati wote ili kubeba dhambi
za wengi;[a] na mara ya pili[b] atakapotokea[c] itakuwa ni bila dhambi[d] na kwa wale wanaomtazamia kwa bidii kwa ajili ya wokovu wao.[e]

10 Kwa kuwa Sheria ina kivuli[f] cha mambo mema
yatakayokuja, lakini si umbo
halisi la mambo hayo, watu hawawezi kamwe kuwafanya
wale wanaokaribia kuwa wakamilifu[g] kwa dhabihu zilezile
mwaka baada ya mwaka ambazo wao huendelea kuzitoa.
2 Kama sivyo, je, dhabihu hazingekoma kutolewa, kwa sababu wale wanaotoa utumishi mtakatifu ambao walikuwa
wamesafishwa mara moja kwa
wakati wote hawangekuwa
na ufahamu wa dhambi tena?[h]
3 Kinyume cha hilo, kwa dhabihu hizo kuna kukumbusha
juu ya dhambi mwaka baada
ya mwaka,[i] **4** kwa maana haiwezekani damu ya ng'ombe na
ya mbuzi kuondolea mbali dhambi.[j]

5 Kwa hiyo wakati yeye anapokuja katika ulimwengu anasema: "'Dhabihu na toleo wewe
hukutaka,[k] bali ulinitayarishia
mwili.[l] **6** Hukukubali matoleo
mazima ya kuteketezwa na toleo la dhambi.'[m] **7** Ndipo nikasema, 'Tazama! Nimekuja (katika kitabu cha kukunjwa imeandikwa juu yangu)[n] ili kufanya mapenzi yako, Ee Mungu.'"[o]
8 Baada ya kwanza kusema:
"Hukutaka wala hukukubali
dhabihu na matoleo na matoleo
mazima ya kuteketezwa na toleo la dhambi"[p]—dhabihu zinazotolewa kulingana na Sheria[q]— **9** ndipo anasema: "Tazama! nimekuja kufanya mapenzi yako."[a] Anaondolea mbali lile
la kwanza ili asimamishe lile la
pili.[b] **10** Kwa hayo "mapenzi"[c]
yaliyosemwa sisi tumetakaswa[d]
kupitia toleo[e] la mwili wa Yesu
Kristo[f] mara moja kwa wakati
wote.

11 Pia, kila kuhani husimama mahali pake[g] siku baada ya
siku[h] ili kutoa utumishi wa watu
wote na kutoa dhabihu zilezile
mara nyingi, kwa kuwa hizo haziwezi kamwe kuondoa kabisa
dhambi.[i] **12** Lakini mtu huyu
alitoa dhabihu moja kwa ajili ya dhambi daima[j] na kuketi kwenye mkono wa kuume wa
Mungu,[k] **13** tangu wakati huo
na kuendelea akingojea mpaka
adui zake wawekwe kuwa kiti
cha miguu yake.[l] **14** Kwa maana ni kwa toleo moja la dhabihu[m] kwamba yeye amewafanya
wale wanaotakaswa wawe wakamilifu[n] daima. **15** Zaidi ya
hayo, roho takatifu[o] pia inatutolea ushahidi, kwa maana baada ya kusema: **16** "'Hili ndilo agano nitakalofanya kwao
baada ya siku hizo,' asema Yehova. 'Nitazitia sheria zangu katika mioyo yao, nami nitaziandika katika akili zao,'"[p] **17** inasema baadaye: "Nami sitazikumbuka tena dhambi zao hata
kidogo na matendo yao ya kuasi sheria."[q] **18** Sasa mahali palipo na msamaha[r] wa mambo
hayo, hapana tena toleo kwa
ajili ya dhambi.[s]

19 Kwa hiyo, akina ndugu,
kwa kuwa tuna ujasiri wa njia
ya kuingia[t] katika mahali patakatifu[u] kwa damu ya Yesu,
20 aliyotuzindulia kuwa njia
mpya na yenye uzima kupitia
lile pazia,[v] yaani, mwili wake,[w]
21 na kwa kuwa tuna kuhani

SURA 9
a Isa 53:12 1Pe 2:24
b Mt 24:3 Tit 2:13
c 2Th 1:7
d Mt 24:30
e Mt 25:34 2Ti 4:8

SURA 10
f Kol 2:17 Ebr 8:5
g Ebr 7:19 Ebr 9:9
h Ga 3:21
i Law 16:30 Law 16:34
j Isa 1:11 Mik 6:7
k Zb 50:8 Amo 5:22
l Zb 40:6
m Zb 40:6
n Zb 40:7
o Zb 40:8
p Zb 40:6
q Law 17:5

Safu ya 2
a Zb 40:8 Yoh 6:38
b Kol 2:14 Ebr 8:13
c Zb 40:8 Ga 1:4
d Yoh 17:19 1Ko 6:11 Ebr 13:12
e Efe 5:2
f Ro 6:10 Ebr 9:28
g 1Sa 2:28 1Nya 24:19 2Nya 29:11
h Kut 29:38 Hes 28:3
i Ebr 7:18 Ebr 7:27 Ebr 10:1
j Ebr 9:28
k Ro 8:34 Kol 3:1
l Zb 110:1 Mdo 2:35 1Ko 15:25
m Ebr 9:28
n Ebr 7:11 Ebr 7:19
o Yer 1:4
p Yer 31:33 Ebr 8:10
q Yer 31:34 Ebr 8:12
r Yoh 8:36
s Yoh 20:23
t Yoh 14:6 Ro 5:2
u Ebr 9:8 Ebr 9:24
v Mt 27:51
w Yoh 6:51 Ebr 6:20

mkuu juu ya nyumba ya Mungu,[a] **22** acheni tukaribie tukiwa na mioyo ya kweli katika uhakikisho kamili wa imani, mioyo yetu ikiisha kunyunyizwa kutokana na dhamiri[b] ya uovu na miili yetu kuoshwa kwa maji safi.[c] **23** Acheni tushike imara tangazo la hadharani la tumaini[d] letu bila kuyumba-yumba,[e] kwa maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu.[f] **24** Na acheni tufikiriane ili kuchocheana[g] katika upendo na matendo mazuri,[h] **25** bila kuacha kukusanyika pamoja sisi wenyewe,[i] kama vile wengine walivyo na desturi, bali tutiane moyo,[j] na kufanya hivyo zaidi kwa kadiri mnavyoona siku ile kuwa inakaribia.[k]

26 Kwa maana tukizoea kutenda dhambi kimakusudi[l] baada ya kupokea ujuzi sahihi juu ya kweli,[m] hakuna tena dhabihu yoyote iliyobaki kwa ajili ya dhambi,[n] **27** lakini kuna tarajio hakika lenye kuogopesha la hukumu[o] na kuna wivu unaowaka moto ambao utawateketeza wale wanaopinga.[p] **28** Mtu yeyote ambaye ameipuuza sheria ya Musa hufa bila huruma, kwa ushuhuda wa watu wawili au watatu.[q] **29** Je, mnafikiri atahesabiwa kuwa anastahili adhabu kali zaidi namna gani,[r] mtu ambaye amemkanyagia chini[s] Mwana wa Mungu na ambaye ameiona kuwa yenye thamani ya kawaida tu damu[t] ya agano ambayo kupitia hiyo alitakaswa, na ambaye ameitendea kwa dharau ile roho[u] ya fadhili zisizostahiliwa? **30** Kwa maana tunamjua yeye aliyesema: "Kisasi ni changu; mimi nitalipa";[v] na tena: "Yehova atawahukumu watu wake."[a] **31** Ni jambo lenye kuogopesha kuanguka mikononi mwa Mungu aliye hai.[b]

32 Hata hivyo, endeleeni kuzikumbuka zile siku za zamani ambazo, baada ya kutiwa nuru,[c] mlivumilia shindano kubwa chini ya mateso,[d] **33** nyakati fulani mkifunuliwa wazi kama katika jumba la maonyesho[e] kwenye shutuma na dhiki pia, na nyakati fulani mlipokuwa washiriki pamoja na wale waliokuwa wakipatwa na jambo la namna hiyo.[f] **34** Kwa maana mliwasikitikia wale waliokuwa gerezani na pia kwa shangwe mkavumilia kuporwa[g] mali zenu, mkijua ninyi wenyewe mna miliki bora na yenye kudumu.[h]

35 Kwa hiyo, msiutupilie mbali uhuru wenu wa kusema,[i] ulio na thawabu[j] kubwa ya kulipwa. **36** Kwa maana mnahitaji kuwa na uvumilivu,[k] ili kwamba, baada ya kufanya mapenzi ya Mungu,[l] mpokee utimizo wa ile ahadi.[m] **37** Kwa maana bado "muda kidogo sana,"[n] na "yeye anayekuja atafika naye hatakawia."[o] **38** "Lakini mwadilifu wangu ataishi kwa sababu ya imani,"[p] na, "akirudi nyuma kwa kutetemeka, nafsi yangu haipendezwi naye."[q] **39** Sasa sisi si namna ya watu wanaorudi nyuma kwenye maangamizi,[r] bali sisi ni namna ya watu walio na imani ya kuihifadhi hai nafsi.[s]

11 Imani[t] ni tarajio lililohakikishwa la mambo yanayotumainiwa,[u] uthibitisho ulio wazi wa mambo halisi ingawa hayaonekani.[v] **2** Kwa

SURA 10
a Zek 6:13; Ebr 3:6
b Ebr 13:18; 1Yo 1:7
c Eze 36:25; Efe 5:26
d Ebr 3:6; Ebr 6:19
e 1Ko 15:58; Kol 1:23
f 1Th 5:24
g Kut 25:2
h Kol 3:23; 1Ti 6:18
i Kum 31:12; Mt 18:20; Mdo 2:42; Mdo 20:8
j Isa 35:3; Ro 1:12
k Ro 13:11; 2Pe 3:12
l Yak 4:17; 1Yo 5:16
m Ebr 6:4; 2Pe 2:21
n Mt 12:32
o Lu 19:27
p Isa 26:11; Mk 3:29
q Kum 17:6
r 1Pe 4:18
s Mt 7:6; Flp 3:18; Ebr 6:6
t Mt 26:28; Lu 22:20
u Efe 4:30
v Kum 32:35

Safu ya 2
a Kum 32:36
b Ebr 12:29; 2Pe 2:4
c Mdo 26:18; 2Ko 4:6; Ebr 6:4
d Flp 1:29; 2Ti 3:12
e 1Ko 4:9
f Flp 1:7
g Mt 5:12
h Lu 16:9
i Yoh 18:20; 1Ko 15:58
j Mt 10:32
k Lu 21:19; Yak 5:11
l Ga 6:9
m Ga 3:29; Kol 3:24
n Isa 26:20
o Hab 2:3; 2Pe 3:9
p Hab 2:4; Yoh 3:16; Ro 1:17
q Hab 2:4; 1Yo 2:19
r 2Pe 2:20
s 1Th 5:9; 1Pe 1:9

SURA 11
t Lu 17:5; Lu 18:8; Ga 3:11
u Ebr 10:22; Ebr 11:13; v Ro 8:24; 2Ko 4:18; 2Ko 5:7.

maana kwa njia ya imani hiyo
watu wa nyakati za zamani wa-
litolewa ushahidi.[a]
3 Kwa imani tunatambua
kwamba mifumo ya mambo[b] ili-
pangwa kwa utaratibu kwa neno
la Mungu,[c] hivi kwamba kile ki-
nachoonekana kimekuja kuto-
kana na vitu visivyoonekana.[d]
4 Kwa imani Abeli alimtolea
Mungu dhabihu ya thamani ku-
bwa zaidi kuliko Kaini,[e] ima-
ni ambayo kupitia hiyo alitole-
wa ushahidi kwamba yeye ali-
kuwa mwadilifu, Mungu akitoa
ushahidi[f] kuhusu zawadi zake;
na kupitia hiyo yeye, ijapoku-
wa alikufa, bado anasema.[g]
5 Kwa imani Enoko[h] alihami-
shwa ili asione kifo, naye ha-
kupatikana popote kwa sababu
Mungu alikuwa amemhamisha;[i]
kwa maana kabla ya kuhami-
shwa kwake alikuwa ametole-
wa ushahidi kwamba amempe-
ndeza Mungu vema.[j] **6** Zaidi
ya hayo, bila imani[k] haiwezeka-
ni kamwe kumpendeza vema,[l]
kwa maana yule anayemkaribia
Mungu lazima aamini kwamba
yeye yuko[m] na kwamba yeye
huwa mthawabishaji[n] wa wale
wanaomtafuta kwa bidii.[o]
7 Kwa imani Noa,[p] baada
ya kupewa onyo la kimungu
la mambo ambayo yalikuwa
bado hayajaonekana,[q] alionye-
sha woga wa kimungu na kuje-
nga safina[r] kwa ajili ya kuiokoa
nyumba yake; na kupitia imani
hiyo aliuhukumu ulimwengu[s]
kuwa wenye hatia, naye akawa
mrithi wa uadilifu[t] unaolinga-
na na imani.
8 Kwa imani Abrahamu,[u]
alipoitwa, alitii kwa kutoka
akaenda na kuingia mahali ali-
pokusudiwa kupokea kuwa
urithi; naye akatoka, ijapoku-
wa hakujua mahali alipokuwa
akienda.[a] **9** Kwa imani ali-
kaa kama mgeni katika nchi ya
ahadi kama katika nchi ya uge-
nini,[b] akakaa katika mahema[c]
pamoja na Isaka[d] na Yakobo,[e]
warithi pamoja naye wa ahadi
ileile.[f] **10** Kwa maana ali-
kuwa akingojea jiji[g] lililo na mi-
singi ya kweli, ambalo mjenzi
na mtengenezaji wa jiji hilo
ni Mungu.[h]
11 Kwa imani Sara[i] mwenye-
we pia alipokea nguvu ili kuchu-
kua mimba ya uzao, hata alipo-
kuwa amepita mpaka wa umri,[j]
kwa kuwa alimwona kuwa mwa-
minifu yeye aliyekuwa ameahi-
di.[k] **12** Kwa sababu hiyo pia
kutoka kwa mwanamume mmo-
ja,[l] naye akiwa kana kwamba ni
mfu,[m] kulizaliwa watoto kama
vile nyota za mbinguni kwa wi-
ngi na kama mchanga ulio ka-
ndo ya bahari, usiohesabika.[n]
13 Katika imani hawa wote
walikufa,[o] ijapokuwa hawaku-
pata utimizo wa zile ahadi,[p] bali
waliziona kwa mbali[q] na kuzi-
karibisha na kutangaza hadha-
rani kwamba wao ni wageni na
wakaaji wa muda katika nchi.[r]
14 Kwa maana wale wanaose-
ma mambo ya namna hiyo hu-
toa uthibitisho wa kwamba wa-
natafuta kwa bidii mahali pao
wenyewe.[s] **15** Na bado, kama
kwa kweli wangeendelea kuku-
mbuka mahali pale walipoku-
wa wametoka,[t] wangepata
nafasi ya kurudi.[u] **16** Lakini
sasa wanajitahidi kufikia ma-
hali palipo bora, yaani, pana-
pohusiana na mbinguni.[v] Kwa
hiyo Mungu haoni aibu juu yao,
kuitwa akiwa Mungu wao,[w]

SURA 11

a Ebr 11:39
b Kol 1:26
c Zb 33:6
2Pe 3:5
d Ro 1:20
e Mwa 4:5
f Mwa 4:4
g Mwa 4:10
Mt 23:35
h Mwa 5:22
Yud 14
i Mwa 5:24
j Mwa 5:22
k 2Th 3:2
l Ga 2:16
m Yoh 7:28
Ro 10:14
Ebr 9:24
n 1Sa 2:7
Zb 58:11
Mt 5:12
o Sef 2:3
Mt 6:33
p Mwa 6:8
q Mwa 6:13
r Mwa 6:14
s Mwa 6:22
t Ro 1:17
Ro 3:22
Ga 5:5
Flp 3:9
2Pe 2:5
u Mwa 12:1
Ro 4:11
Ro 4:13

Safu ya 2

a Mwa 12:4
Mdo 7:2
b Mwa 23:4
c Mwa 12:8
d Mwa 21:3
e Mwa 25:26
f Mwa 17:6
Mwa 26:3
Mwa 28:13
g Yoh 8:56
Ebr 13:14
Ufu 21:2
h Ebr 3:4
i Mwa 17:15
j Mwa 17:17
k Mwa 21:2
l Mwa 21:5
m Ro 4:19
n Mwa 22:17
1Fa 4:20
o Mwa 23:4
p Mwa 47:9
q Yoh 8:56
r 1Nya 29:15
Zb 39:12
Efe 2:19
1Pe 2:11
s Ebr 13:14
t Mwa 11:31
u Mwa 24:6
v Mt 4:17
Mt 25:34
Flp 3:20
w Kut 3:15
Mt 22:32
Mdo 7:32

kwa maana ametayarisha jiji[a]
kwa ajili yao.
17 Kwa imani Abrahamu,
alipojaribiwa,[b] ni kana kwamba
alimtoa Isaka, na huyo mtu
aliyekuwa amezipokea aha-
di kwa furaha alijaribu kumtoa
mwana wake mzaliwa-pekee,[c]
18 ijapokuwa alikuwa amea-
mbiwa: "Ule utakaoitwa 'uzao
wako' utakuwa kupitia Isaka."[d]
19 Lakini alifikia uamuzi kwa-
mba Mungu alikuwa na uwezo
wa kumfufua hata kutoka kwa
wafu;[e] na kutoka huko alimpo-
kea pia kwa njia ya mfano.[f]
20 Kwa imani pia Isaka ali-
mbariki Yakobo[g] na Esau[h] ku-
husu mambo yatakayokuja.
21 Kwa imani Yakobo, alipo-
kuwa karibu kufa,[i] aliwabariki
kila mmoja wa wana wa Yosefu[j]
na kuabudu akiegemea juu ya
fimbo yake.[k]
22 Kwa imani Yosefu, akika-
ribia mwisho wake, alitaja ku-
husu kule kutoka[l] kwa wana wa
Israeli; naye akatoa amri kuhu-
su mifupa yake.[m]
23 Kwa imani Musa alifichwa
kwa miezi mitatu na wazazi
wake baada ya kuzaliwa kwa-
ke,[n] kwa sababu waliona kwa-
mba huyo mtoto mchanga aliku-
wa mwenye kupendeza[o] nao ha-
wakuliogopa agizo[p] la mfalme.
24 Kwa imani Musa, alipoku-
wa mtu mzima,[q] alikataa kui-
twa mwana wa binti ya Farao,[r]
25 akachagua kutendewa vi-
baya pamoja na watu wa Mu-
ngu badala ya kufurahia dha-
mbi kwa muda, **26** kwa saba-
bu aliona shutuma ya Kristo[s]
kuwa ni utajiri mkubwa kuliko
hazina za Misri; kwa maana ali-
kaza macho kwenye malipo ya
thawabu.[t] **27** Kwa imani alio-
ndoka Misri,[a] lakini bila kuogo-
pa hasira ya mfalme,[b] kwa maa-
na aliendelea kuwa imara kama
mtu anayemwona Yeye asiyeo-
nekana.[c] **28** Kwa imani alifa-
nya sherehe ya pasaka[d] na upa-
kaji wa damu,[e] ili mwangami-
zaji asiwaguse wazaliwa wao wa
kwanza.[f]
29 Kwa imani walipita kati-
kati ya Bahari Nyekundu kana
kwamba ni juu ya nchi kavu,[g]
lakini Wamisri walipothubutu
kuipitia wakamezwa.[h]
30 Kwa imani kuta za Ye-
riko zilianguka chini baada ya
kuzungukwa kwa siku saba.[i]
31 Kwa imani Rahabu[j] yule ka-
haba hakuangamia pamoja na
wale waliotenda kwa kutotii,
kwa sababu aliwapokea wale
wapelelezi kwa njia ya amani.[k]
32 Nami nitasema nini zai-
di? Kwa maana nitakosa wa-
kati nikiendelea kusimulia juu
ya Gideoni,[l] Baraka,[m] Samso-
ni,[n] Yeftha,[o] Daudi[p] na vile-
vile Samweli[q] na wale mana-
bii wengine,[r] **33** ambao ku-
pitia imani walishinda falme
katika mapambano,[s] wakate-
nda uadilifu,[t] wakapata ahadi,[u]
wakaziba vinywa vya simba,[v]
34 wakazuia nguvu za moto,[w]
wakaponyoka makali ya upa-
nga,[x] kutoka hali ya udhaifu
wakafanywa kuwa wenye ngu-
vu,[y] wakawa mashujaa katika
vita,[z] wakayashinda kabisa ma-
jeshi ya wageni.[a] **35** Wana-
wake waliwapokea wafu wao
kwa ufufuo;[b] lakini watu wengi-
ne waliteswa kwa sababu ha-
wakukubali kuachiliwa huru
kupitia fidia fulani, ili waupa-
te ufufuo ulio bora. **36** Ndiyo,
wengine walipata jaribu lao
kwa dhihaka na mapigo kwa

SURA 11
a Ebr 12:22
Ufu 21:2
b Mwa 22:1
c Mwa 22:9
Yoh 3:16
d Mwa 21:12
Ro 9:7
e Ro 4:17
f 1Ko 10:11
1Ko 15:20
g Mwa 27:27
h Mwa 27:39
i Mwa 47:29
j Mwa 48:20
k Mwa 47:31
l Mwa 50:24
m Mwa 50:25
Kut 13:19
n Kut 2:2
o Mdo 7:20
p Kut 1:16
Kut 1:22
q Kut 2:11
r Kut 2:10
Mdo 7:21
s Zb 69:9
Ro 15:3
t Ebr 10:34

Safu ya 2
a Kut 12:51
b Kut 10:28
c Yoh 1:18
Yoh 4:24
1Ti 1:17
d Kut 12:21
e Kut 12:22
f Kut 12:23
g Kut 14:22
h Kut 14:28
i Yos 6:20
j Yos 2:1
k Yos 6:17
l Amu 6:11
m Amu 4:6
n Amu 13:24
o Amu 11:1
p 1Sa 16:13
q 1Sa 3:20
r Mdo 3:24
s Amu 7:22
t Mwa 15:6
Ebr 11:4
u 2Sa 7:12
v Amu 14:6
1Sa 17:34
w Da 3:23
x 2Fa 6:15
y Amu 16:28
1Fa 18:46
z Amu 11:32
2Sa 23:8
a Amu 4:16
b 1Fa 17:22
2Fa 4:34

mijeledi, kwa kweli, zaidi
ya hayo, kwa vifungo[a] na ma-
gereza.[b] **37** Walipigwa kwa
mawe,[c] walijaribiwa,[d] walika-
twa vipande-vipande kwa msu-
meno, walikufa[e] kwa kuua-
wa kwa upanga, walitembea
huku na huku wakiwa wame-
vikwa ngozi za kondoo,[f] waki-
wa wamevikwa ngozi za mbu-
zi, wakiwa katika uhitaji,[g] kati-
ka dhiki,[h] wakitendewa vibaya;[i]
38 na ulimwengu haukuwafaa.
Walitembea huku na huku kati-
ka majangwa na milima na ma-
pango[j] na mashimo ya dunia.

39 Na bado hawa wote, ijapo-
kuwa walitolewa ushahidi ku-
pitia imani yao, hawakupata
utimizo wa ile ahadi,[k] **40** kwa
kuwa Mungu aliona kimbele
kitu bora[l] kwa ajili yetu sisi,[m] ili
wasifanywe[n] kuwa wakamilifu[o]
bila sisi.[p]

12 Kwa hiyo, basi, kwa sa-
babu tuna wingu kubwa
hivyo la mashahidi[q] linalotuzu-
nguka, acheni sisi pia tuondoe
kila uzito[r] na dhambi ambayo
hututatanisha kwa urahisi,[s] na
acheni tukimbie kwa uvumili-
vu[t] shindano la mbio[u] lililowe-
kwa mbele yetu,[v] **2** huku tu-
kimtazama kwa makini Waki-
li Mkuu[w] na Mkamilishaji wa
imani yetu,[x] Yesu. Kwa ajili
ya shangwe iliyowekwa mbele
yake, yeye alivumilia[y] mti wa
mateso, akaidharau aibu, naye
ameketi kwenye mkono wa ku-
ume wa kiti cha ufalme cha
Mungu.[z] **3** Kwa kweli, mfikiri-
rieni sana yeye ambaye ame-
vumilia maneno ya aina hii
yenye kupinga[a] yanayotolewa
na watenda-dhambi kinyume
cha faida zao wenyewe, ili ni-

SURA 11

a Yer 20:2
b Yer 37:15
c 1Fa 21:13
2Nya 24:21
d 1Fa 22:24
e 1Fa 18:4
f 2Fa 1:8
g 1Fa 19:5
h 1Fa 19:2
i Yer 38:6
j 1Fa 18:4
1Fa 19:9
k Mwa 22:18
Mwa 49:10
Ebr 11:13
l Ro 8:18
Ro 9:27
Ro 11:5
Ebr 10:19
m Ebr 2:3
Ebr 3:1
Ebr 7:22
Ufu 20:6
n Ebr 11:32
o Ebr 7:11
Ebr 7:19
p Yak 1:18
Ufu 14:4

SURA 12

q Ebr 11:39
r 1Ko 9:26
Flp 3:13
1Pe 2:1
s Kol 2:8
1Ti 6:9
Ebr 3:12
t 1Ti 6:12
u 1Ko 9:24
v Flp 3:14
w Yoh 14:6
Mdo 5:31
Ebr 2:10
x 1Ko 1:8
Flp 1:6
y Flp 2:8
z Zb 110:1
Ebr 10:12
a Mt 27:39

Safu ya 2

a Ga 6:9
2Th 3:13
b Mdo 12:2
Ebr 10:32
c Mt 5:45
d Met 3:11
e Met 3:12
f Ebr 12:1
g 2Sa 7:14
Mt 5:9
Ebr 2:10
h Met 13:24
i Kum 23:2
j Met 23:13
k Hes 16:22
Isa 42:5
Mal 1:6
Yak 4:10
l Met 22:6
m Law 11:44
1Pe 1:15
n 2Ko 4:17
o 1Pe 1:6
p Flp 1:11
Yak 3:18
q Ayu 4:3
Isa 40:29
Lu 22:32
r Isa 35:3
naye akapewa mamlaka ya ku-
tenda kwa miezi 42.[j] **6** Naye
akafungua kinywa chake kwa
kumkufuru[k] Mungu, kulikufu-
ru jina lake na makao yake,
hata wale wanaokaa mbinguni.[l]
7 Naye akapewa ruhusa[m] ya ku-
pigana vita na watakatifu na ku-
washinda,[n] naye akapewa ma-
mlaka juu ya kila kabila na watu
na lugha na taifa. **8** Na wale
wote wanaokaa duniani wata-
mwabudu; hakuna jina la hata
mmoja wao limeandikwa katika
kitabu cha kukunjwa[o] cha uzi-
ma cha Mwana-Kondoo aliye-
chinjwa,[p] tangu kuwekwa msi-
ngi wa ulimwengu.[q]
9 Ikiwa yeyote ana sikio, na
asikie.[r] **10** Ikiwa yeyote ame-
kusudiwa kwenda utekwani,
yeye huenda zake utekwani.[a]
Ikiwa yeyote ataua kwa upa-
nga, yeye lazima atauawa kwa
upanga.[b] Hapa ndipo panapo-
maanisha uvumilivu[c] na imani[d]
ya watakatifu.[e]
11 Nami nikamwona mnya-
ma-mwitu[f] mwingine akipa-
nda kutoka katika dunia,[g] naye
alikuwa na pembe mbili kama
mwana-kondoo, lakini akaanza
kusema kama joka[h] mkubwa.
12 Naye anatumia mamlaka
yote ya yule mnyama-mwitu[i]
wa kwanza machoni pake. Naye
huifanya dunia na wale wana-
okaa ndani yake wamwabudu
yule mnyama-mwitu wa kwa-
nza, ambaye pigo lake la kifo lili-
pona.[j] **13** Naye hufanya isha-
ra[k] kubwa, hivi kwamba hata
yeye hufanya moto ushuke ku-
toka mbinguni mpaka duniani
machoni pa wanadamu.
14 Naye huwapotosha wale
wanaokaa duniani, kwa sababu
ya ishara alizopewa ruhusa ku-
fanya machoni pa yule mnya-
ma-mwitu, huku akiwaambia
wale wanaokaa duniani wafa-
nye sanamu[l] ya yule mnyama-
mwitu aliyekuwa na pigo[m] la
upanga na bado akarudi kwe-
nye uzima. **15** Naye akapewa
ruhusa kuipa pumzi ile sanamu
ya mnyama-mwitu, hivi kwa-
mba ile sanamu ya mnyama-
mwitu iseme na pia kufanya wa-
uawe wale wote ambao hawaku-
taka hata kidogo kuiabudu ile
sanamu[n] ya mnyama-mwitu.
16 Naye huwalazimisha watu
wote,[o] wadogo kwa wakubwa,
na matajiri kwa maskini, na wa-
lio huru kwa watumwa, kwa-
mba wawape hao alama katika
mkono wao wa kuume au juu

SURA 13
a Zb 74:10
b Da 7:6
c Da 7:5
d Da 7:4
e Ufu 12:9
f Lu 4:6
g Ufu 13:14
h Da 7:8
i Lu 12:10
j Ufu 11:2
Ufu 11:3
k Kut 5:2
Isa 14:13
Da 7:25
l Ufu 12:12
m Yoh 19:11
n Lu 22:31
Ufu 12:17
o Da 12:1
Ufu 3:5
Ufu 21:27
p Isa 53:7
Mt 27:50
Ufu 5:6
Ufu 5:12
q Efe 1:4
1Pe 1:20
r Mt 11:15

Safu ya 2
a Zek 14:2
b Mwa 9:6
Mt 26:52
c Mt 24:13
Ebr 10:36
Ebr 12:3
d Ufu 2:10
e Da 7:18
1Ko 6:2
Ufu 20:6
f Da 7:8
Ufu 16:13
Ufu 19:20
g Ufu 12:16
h Da 7:8
Ufu 16:13
Ufu 20:2
i Ufu 13:1
j Ufu 13:3
k Kum 13:1
Mt 24:24
l Kut 20:4
Ufu 19:20
Ufu 20:4
m Ufu 13:3
n Kum 29:17
1Fa 11:5
Da 3:6
Mt 24:15
o Yer 39:10
Yer 52:16

ya paji la uso wao,[a] **17** na kwamba mtu yeyote asiweze kununua au kuuza isipokuwa mtu aliye na ile alama, jina[b] la yule mnyama-mwitu au namba ya jina lake.[c] **18** Hapa ndipo hekima inapohitajiwa: Yeye aliye na akili na apige hesabu ya namba ya yule mnyama-mwitu, kwa maana ni namba ya mwanadamu;[d] na namba yake ni 666.[e]

14 Nami nikaona, na, tazama! Mwana-Kondoo[f] amesimama juu ya Mlima Sayuni,[g] na pamoja naye 144,000[h] wakiwa na jina lake na jina la Baba[i] yake limeandikwa juu ya mapaji ya nyuso zao. **2** Nami nikasikia sauti kutoka mbinguni kama sauti ya maji mengi[j] na kama sauti ya ngurumo kubwa; na sauti niliyosikia ilikuwa kama ya waimbaji ambao wanafuatanisha sauti zao kwa kinubi[k] wakivipiga vinubi vyao. **3** Nao wanaimba[l] kana kwamba ni wimbo mpya[m] mbele ya kile kiti cha ufalme na mbele ya wale viumbe hai wanne[n] na wale wazee;[o] na hakuna yeyote aliyeweza kujifunza kikamili wimbo ule ila wale 144,000,[p] ambao wamenunuliwa[q] kutoka duniani. **4** Hao ndio wale ambao hawakujitia unajisi na wanawake;[r] kwa kweli, wao ni mabikira.[s] Hao ndio wale wanaoendelea kumfuata Mwana-Kondoo popote anapoenda.[t] Hao walinunuliwa[u] kutoka kati ya wanadamu wakiwa matunda ya kwanza[v] kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo, **5** na hamna uwongo uliopatikana katika vinywa vyao;[w] wao hawana dosari.[x]

SURA 13
a Ufu 14:9; Ufu 16:2; Ufu 19:20
b Ufu 14:11
c Ufu 15:2
d Mhu 7:20; Ro 3:23
e 1Nya 20:6; Da 3:1

SURA 14
f Yoh 1:29; Ufu 5:6; Ufu 22:3
g Zb 2:6; Ebr 12:22; 1Pe 2:6
h Ufu 7:4
i Ufu 3:12
j Ufu 1:15
k 2Nya 5:12; Ufu 5:8
l 1Nya 6:31
m Zb 33:3; Zb 98:1; Zb 149:1; Ufu 5:9
n Ufu 4:6
o Ufu 4:4; Ufu 19:4
p Ufu 7:4; Ufu 14:1
q 1Ko 6:20
r Yak 1:27
s 2Ko 11:2; Yak 4:4
t 1Pe 2:21
u 1Ko 7:23; Ufu 5:9
v Kut 23:16; Law 23:15; Yak 1:18
w Met 14:5; Ufu 21:27
x Efe 5:27; Yud 24

Safu ya 2
a Kum 4:11; Ufu 8:13; Ufu 19:17
b Mt 24:14; Mk 13:10
c Mdo 1:8; Kol 1:23
d Met 8:13; Mt 10:28
e Zb 19:1; Ro 11:36; Yud 25; Ufu 4:9
f 1Pe 4:17; 2Pe 2:9
g Kut 20:11; Zb 124:8; Zb 146:6
h Mdo 14:15
i Ufu 17:18; Ufu 18:2
j Isa 21:9; Yer 51:8; Ufu 18:21
k Yer 51:7
l Ufu 17:2; Ufu 18:3
m Ufu 13:1
n Ufu 13:15
o Ufu 13:16
p Zb 75:8; Ufu 11:18; Ufu 16:19
q Ufu 20:10
r Ufu 21:8

6 Nami nikamwona malaika mwingine akiruka katikati ya mbingu,[a] naye alikuwa na habari njema[b] ya milele ili aitangaze kuwa habari za furaha kwa wale wanaokaa duniani, na kwa kila taifa na kabila na lugha na watu,[c] **7** akisema kwa sauti kubwa: "Mwogopeni Mungu[d] na kumpa utukufu,[e] kwa sababu saa ya hukumu yake imefika,[f] na kwa hiyo mwabuduni Yeye aliyezifanya[g] mbingu na dunia na bahari na chemchemi za maji."[h]

8 Na mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema: "Ameanguka! Babiloni[i] Mkubwa ameanguka,[j] yeye aliyeyafanya mataifa yote yanywe kutokana na divai[k] ya hasira ya uasherati wake!"[l]

9 Na malaika mwingine, wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kubwa: "Yeyote akimwabudu yule mnyama-mwitu[m] na sanamu yake,[n] na kupokea alama juu ya paji la uso wake au juu ya mkono wake,[o] **10** yeye pia atakunywa kutokana na divai ya hasira ya Mungu inayomwagwa bila kuchanganywa na kitu ndani ya kikombe cha ghadhabu yake,[p] naye atateswa[q] kwa moto na kiberiti[r] machoni pa malaika watakatifu na machoni pa Mwana-Kondoo. **11** Na moshi wa kuteswa kwao unapanda milele na milele,[s] nao hawana pumziko mchana na usiku, wale wanaomwabudu yule mnyama-mwitu na sanamu yake, na yeyote anayepokea alama[t] ya jina lake. **12** Hapa ndipo panapomaanisha uvumi-

s Mt 25:46; 2Th 1:9; Ufu 19:3; t Ufu 13:16; Ufu 16:2; Ufu 20:4.

livu kwa watakatifu,[a] wale wanaoshika amri za Mungu[b] na imani[c] kwa Yesu."

13 Nami nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema: "Andika: Wenye furaha ni wafu[d] wanaokufa katika muungano na Bwana[e] tangu wakati huu na kuendelea.[f] Ndiyo, roho inasema, acheni wapumzike kutokana na kazi zao za jasho, kwa maana mambo waliyotenda yanaambatana nao moja kwa moja."

14 Nami nikaona, na, tazama! wingu jeupe, na mtu fulani kama mwana wa binadamu[g] ameketi juu ya wingu lile, mwenye taji la dhahabu[h] juu ya kichwa chake na mundu mkali mkononi mwake.

15 Na malaika mwingine akatokea katika patakatifu pa hekalu, akimpaazia sauti kubwa yule anayeketi juu ya lile wingu: "Tia ndani mundu wako uvune,[i] kwa sababu saa imekuja ya kuvuna, kwa maana mavuno[j] ya dunia yameiva kabisa."[k] **16** Na yule aliyeketi juu ya wingu akatia ndani mundu wake duniani, nayo dunia ikavunwa.

17 Na bado malaika mwingine akatokea katika patakatifu pa hekalu palipo mbinguni,[l] yeye, pia, akiwa na mundu mkali.

18 Na bado malaika mwingine akatokea katika madhabahu naye alikuwa na mamlaka juu ya moto.[m] Naye akapaaza sauti kubwa akamwita yule aliyekuwa na mundu mkali, akisema: "Tia ndani mundu wako mkali ukusanye vishada vya mzabibu wa dunia,[n] kwa sababu zabibu zake zimeiva." **19** Na yule malaika[o] akatia ndani mundu wake katika dunia na kukusanya mzabibu[a] wa dunia, naye akautupa ndani ya shinikizo kubwa la divai la hasira ya Mungu.[b] **20** Na lile shinikizo la divai likakanyagiwa nje ya jiji,[c] na damu ikatoka katika lile shinikizo la divai hata kufikia juu kwenye lijamu za farasi,[d] kwa umbali wa stadia elfu moja mia sita.[e]

15 Nami nikaona ishara[f] nyingine mbinguni, kubwa na ya ajabu sana, malaika saba[g] wenye mapigo saba.[h] Hayo ndiyo ya mwisho, kwa sababu kupitia hayo hasira[i] ya Mungu inamalizika.[j]

2 Nami nikaona kitu mfano wa bahari[k] kama kioo iliyochangamana na moto, na wale wanaotokea wakiwa washindi[l] kutoka kwa yule mnyama-mwitu na kutoka kwa ile sanamu[m] yake na kutoka kwa ile namba[n] ya jina lake wakiwa wamesimama kando ya ule mfano wa bahari[o] kama kioo, wakiwa na vinubi[p] vya Mungu. **3** Nao wanaimba wimbo wa Musa[q] mtumwa wa Mungu na wimbo wa Mwana-Kondoo,[r] wakisema:

"Matendo yako ni makuu na ya ajabu,[s] Yehova Mungu, Mweza-Yote.[t] Njia zako ni za uadilifu na za kweli,[u] Mfalme wa umilele.[v] **4** Ni nani ambaye kwa kweli hatakuogopa wewe,[w] Yehova,[x] na kulitukuza jina lako,[y] kwa sababu wewe peke yako ni mshikamanifu?[z] Kwa maana mataifa yote yatakuja na kuabudu mbele zako,[a] kwa sababu amri zako za uadilifu zimefunuliwa."[b]

5 Na baada ya mambo haya nikaona, na patakatifu pa

SURA 14

a Ufu 13:10
b Mhu 12:13
Ufu 1:3
c Ebr 10:38
d Kol 3:3
e Ro 6:3
1Ko 15:51
f 1Th 4:16
g Da 7:13
Mt 25:31
Mdo 1:11
Ufu 1:7
h Zb 21:3
Ufu 6:2
i Mk 4:29
j Mt 13:39
k Yoe 3:13
l Ufu 11:19
m Ufu 20:9
n Kum 32:32
o Mt 13:39
Ufu 9:11

Safu ya 2

a Yer 12:10
b Ufu 19:15
c Ebr 13:12
Ufu 22:15
d Met 21:31
e Yer 25:33

SURA 15

f Ufu 1:1
g Ufu 16:1
h Law 26:21
i Zb 7:11
j Ufu 16:17
k 1Fa 7:23
1Fa 7:39
l Ufu 2:7
m Ufu 13:15
n Ufu 13:18
o Ufu 4:6
p Ufu 5:8
q Kut 15:1
Kum 31:30
Ebr 3:5
r Yoh 1:29
Mdo 3:22
Ebr 2:12
s Kut 15:11
Zb 92:5
Zb 111:2
Zb 139:14
t Kut 6:3
Ufu 19:6
u Kum 32:4
Zb 145:17
v Yer 10:10
1Ti 1:17
w Yer 10:7
x Zb 22:23
Zb 33:8
y Zb 86:12
Yoh 12:28
z Yer 3:12
a Zb 86:9
Mal 1:11
b Isa 2:4

hema[a] la ushahidi[b] pakafunguliwa mbinguni,[c] **6** na wale malaika saba[d] wenye mapigo saba[e] wakatokea katika patakatifu, wamevikwa kitani safi,[f] chenye kung'aa nao wamefungwa vifuani mwao mishipi ya dhahabu. **7** Na mmoja wa wale viumbe hai wanne[g] akawapa wale malaika saba mabakuli saba ya dhahabu yaliyojaa hasira ya Mungu,[h] anayeishi milele na milele.[i] **8** Na patakatifu pakajawa na moshi kwa sababu ya utukufu wa Mungu[j] na kwa sababu ya nguvu zake, na hakuna yeyote aliyeweza kuingia katika patakatifu mpaka yalipomalizika yale mapigo saba[k] ya wale malaika saba.

16 Nami nikasikia sauti[l] kubwa kutoka katika patakatifu ikiwaambia wale malaika saba: "Nendeni mkamwage yale mabakuli saba ya hasira[m] ya Mungu ndani ya dunia."

2 Na yule wa kwanza[n] akaenda zake na kumwaga bakuli lake ndani ya dunia.[o] Na kidonda chenye kuumiza na kilicho hatari[p] kikaja juu ya wale wanadamu waliokuwa na alama ya yule mnyama-mwitu[q] na waliokuwa wakiiabudu sanamu yake.[r]

3 Na yule wa pili[s] akamwaga bakuli lake ndani ya bahari.[t] Nayo ikawa damu[u] kama ya mwanadamu aliyekufa, na kila nafsi iliyo hai ikafa, ndiyo, vitu vilivyo ndani ya bahari.[v]

4 Na yule wa tatu[w] akamwaga bakuli lake ndani ya mito[x] na chemchemi za maji. Nazo zikawa damu.[y] **5** Nami nikamsikia malaika aliye juu ya maji akisema: "Wewe, Ambaye uko na uliyekuwako,[z] Mshikamanifu,[a] wewe ni mwadilifu, kwa sababu umetoa maamuzi haya,[b] **6** kwa sababu waliimwaga damu ya watakatifu na ya manabii,[c] nawe umewapa damu[d] wanywe. Wanastahili hilo."[e] **7** Nami nikaisikia madhabahu ikisema: "Ndiyo, Yehova Mungu, Mweza-Yote,[f] maamuzi yako ya hukumu ni ya kweli na ya uadilifu."[g]

8 Na yule wa nne[h] akamwaga bakuli lake juu ya jua; na jua likapewa ruhusa ya kuwaunguza[i] wanadamu kwa moto. **9** Na wale wanadamu wakaunguzwa kwa joto kubwa, lakini wakalikufuru jina[j] la Mungu, aliye na mamlaka[k] juu ya mapigo haya, nao hawakutubu ili wampe utukufu.[l]

10 Na yule wa tano akamwaga bakuli lake juu ya kiti cha ufalme cha yule mnyama-mwitu.[m] Na ufalme wake ukatiwa giza,[n] nao wakaanza kuzitafuna ndimi zao kwa sababu ya maumivu yao, **11** lakini wakamkufuru[o] Mungu wa mbinguni kwa sababu ya maumivu yao na kwa sababu ya vidonda vyao, nao hawakutubu matendo yao.

12 Na yule wa sita[p] akamwaga bakuli lake juu ya mto mkubwa Efrati,[q] na maji yake yakakauka,[r] ili njia itayarishwe kwa ajili ya wafalme[s] wanaotoka mashariki.

13 Nami nikaona maneno machafu matatu yaliyoongozwa na roho[t] ambayo yalionekana kama vyura[u] yakitoka katika kinywa cha yule joka[v] mkubwa na kutoka katika kinywa cha yule mnyama-mwitu[w] na kutoka katika kinywa cha yule nabii wa uwongo.[x]

SURA 15

a Ebr 8:2; Ebr 9:11
b Mdo 7:44
c Ufu 11:19
d Ufu 8:2
e Ufu 15:1
f Da 10:5
g Ufu 19:4
h Zb 75:8; Yer 25:15; Ufu 14:10
i Zb 90:2; 1Ti 1:17
j Kut 40:34; 1Fa 8:11; Isa 6:4; Eze 44:4
k Law 26:21; Ufu 15:1

SURA 16

l Isa 66:6; Ufu 16:17
m Zb 69:24; Sef 3:8
n Ufu 8:7
o Ufu 20:11
p Kut 9:10; Kum 28:35
q Ufu 13:16; Ufu 13:18
r Ufu 13:15; Ufu 19:20
s Ufu 8:8
t Ufu 17:15
u Kut 7:20
v Isa 57:20
w Ufu 8:10
x Zb 78:44
y Kut 7:20
z Kut 3:14; Ufu 1:4

Safu ya 2

a Zb 145:17; Yer 3:12; Ufu 15:4
b Kum 32:4; Zb 119:137
c Mwa 9:5; Zb 79:3; Mt 23:35
d Isa 49:26
e Ufu 18:20
f Kut 6:3
g Zb 19:9; Zb 119:137; Ufu 19:2
h Ufu 8:12
i Isa 49:10
j Zb 83:18
k Ro 13:1
l Ufu 9:21; Ufu 14:7
m Ufu 13:1
n Kut 10:21; Isa 8:22; Efe 4:18
o Ufu 16:21
p Ufu 9:13
q Zb 137:1
r Isa 44:27; Yer 50:38
s Isa 44:28; Yer 51:57
t 1Yo 4:1
u Law 11:12
v Ufu 12:3
w Ufu 13:1
x Ufu 13:11

14 Hayo, kwa kweli, ni manenо yanayoongozwa[a] na roho waovu nayo yanafanya ishara,[b] nayo yanakwenda kwa wafalme[c] wa dunia nzima inayokaliwa,[d] ili kuwakusanya pamoja kwa vita[e] vya ile siku kuu[f] ya Mungu Mweza-Yote.[g]

15 "Tazama! Ninakuja kama mwizi.[h] Mwenye furaha ni yule anayekaa macho[i] na kutunza mavazi yake ya nje, ili asipate kutembea akiwa uchi na watu waitazame aibu yake."[j]

16 Nayo yakawakusanya pamoja mahali panapoitwa katika Kiebrania Har-Magedoni.[k]

17 Na yule wa saba akamwaga bakuli lake juu ya hewa.[l] Ndipo sauti[m] kubwa ikatokea katika patakatifu kutoka katika kile kiti cha ufalme, ikisema: "Imekuwa!" **18** Na umeme na sauti na ngurumo zikatokea, na kukatokea tetemeko kubwa la nchi[n] la namna ambayo haijatokea tangu wanadamu walipokuja kuwa duniani,[o] tetemeko la nchi[p] lenye kuenea sana, lililo kubwa sana. **19** Na lile jiji kubwa[q] likapasuka na kuwa sehemu tatu, na majiji ya mataifa yakaanguka; na Babiloni Mkubwa[r] akakumbukwa machoni pa Mungu, ili kumpa kikombe cha divai cha hasira ya ghadhabu yake.[s] **20** Pia, kila kisiwa kikakimbia, na milima haikupatikana.[t] **21** Na mvua kubwa ya mawe[u] iliyo na kila jiwe lenye uzito wa karibu talanta moja ikashuka kutoka mbinguni juu ya wanadamu, na wale wanadamu wakamkufuru[v] Mungu kwa sababu ya lile pigo la mvua ya mawe,[w] kwa sababu pigo lake lilikuwa kubwa isivyo kawaida.

SURA 16

a 1Ti 4:1
b Ufu 13:13
c Zb 2:2
d Ufu 18:3
Ufu 18:9
e Eze 38:16
Ufu 19:19
f Yoe 2:1
g Isa 13:6
Yer 25:33
Eze 30:3
Yoe 1:15
Yoe 2:11
Sef 1:15
2Pe 3:12
h 1Th 5:2
2Pe 3:10
i Lu 21:36
j Ufu 3:18
k 2Nya 35:22
Zek 12:11
Ufu 19:19
l Efe 2:2
Efe 6:12
m Isa 66:6
Ufu 16:1
n Eze 38:19
o Da 12:1
p Ebr 12:26
q Ufu 17:18
r Ufu 18:2
s Yer 25:15
Ufu 15:7
t Ufu 6:14
u Ayu 38:22
Ayu 38:23
Isa 28:2
v Ufu 16:9
w Kut 9:24
Ufu 11:19

Safu ya 2

SURA 17

a Ufu 16:1
b 1Ko 6:15
Yak 4:4
c Isa 57:20
Yer 51:13
Ufu 17:15
Ufu 19:2
d Isa 47:5
Yak 4:4
Ufu 18:9
e Yer 51:7
Ufu 14:8
Ufu 18:3
f Eze 37:1
Ufu 1:10
g Ufu 13:15
h Mk 3:29
i Ufu 17:9
j Da 5:29
Lu 16:19
k Mt 27:28
l Ufu 18:12
Ufu 18:19
m Yer 51:7
n Kum 29:17
Isa 66:3
o Ro 1:24
p 2Th 2:7
q Ufu 19:2
r Eze 22:2
Ufu 18:5
s Ufu 18:24
Ufu 19:2
t Ufu 6:9
u Eze 28:19
v Ufu 17:5
w Ufu 17:3
x Ufu 13:15

17 Na mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na mabakuli saba[a] akaja, akasema nami, akaniambia: "Njoo, nitakuonyesha hukumu juu ya yule kahaba[b] mkubwa anayekaa juu ya maji mengi,[c] **2** ambaye wafalme wa dunia walifanya uasherati naye,[d] na wale ambao hukaa katika dunia walileweshwa kwa divai ya uasherati wake."[e]

3 Naye akanichukua katika nguvu za roho[f] kuingia nyikani. Nami nikamwona mwanamke ameketi juu ya mnyama-mwitu[g] mwenye rangi nyekundu aliyejaa majina ya makufuru[h] na aliyekuwa na vichwa saba[i] na pembe kumi. **4** Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo za rangi ya zambarau[j] na nyekundu,[k] naye alikuwa amepambwa dhahabu na jiwe la thamani na lulu[l] na mkononi mwake alikuwa na kikombe cha dhahabu[m] kilichojaa machukizo[n] na mambo machafu ya uasherati wake.[o] **5** Na juu ya paji la uso wake jina, fumbo,[p] lilikuwa limeandikwa: "Babiloni Mkubwa, mama wa makahaba[q] na wa machukizo ya dunia."[r] **6** Nami nikaona kwamba yule mwanamke amelewa damu[s] ya watakatifu na damu ya mashahidi wa Yesu.[t]

Basi, nilipomwona nilishangaa kwa mshangao mkubwa.[u] **7** Na kwa hiyo yule malaika akaniambia: "Kwa nini ulishangaa? Nitakuambia fumbo la yule mwanamke[v] na la yule mnyama-mwitu anayembeba na aliye na vichwa saba na pembe kumi:[w] **8** Mnyama-mwitu uliyemwona alikuwako,[x] lakini hayuko, na bado yuko karibu

kupanda kutoka katika abiso,[a]
naye ataenda kwenye uharibifu. Na watakapoona jinsi yule
mnyama-mwitu alivyokuwako,
lakini hayuko, na bado atakuwapo, wale wanaokaa duniani
watamsifu kwa mshangao, lakini majina yao hayakuandikwa kwenye kile kitabu cha
kukunjwa cha uzima[b] tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu.[c]

9 "Hapa ndipo inapohitajiwa akili yenye hekima:[d] Vile vichwa saba[e] vinamaanisha milima saba,[f] ambapo yule mwanamke huketi juu. **10** Na kuna
wafalme saba: watano wameanguka,[g] mmoja yuko,[h] yule
mwingine bado hajafika,[i] lakini atakapofika lazima adumu
kwa muda mfupi.[j] **11** Na yule
mnyama-mwitu aliyekuwako
lakini hayuko,[k] yeye mwenyewe pia ni mfalme wa nane, lakini anatokana na wale saba,
naye anaenda zake kwenye uharibifu.

12 "Na zile pembe kumi ulizoona zinamaanisha wafalme
kumi,[l] ambao bado hawajapokea ufalme, lakini wanapokea mamlaka wakiwa wafalme saa moja pamoja na yule
mnyama-mwitu. **13** Hawa
wana wazo moja, na kwa hiyo
wanampa yule mnyama-mwitu
nguvu na mamlaka yao.[m]
14 Hawa watapigana na Mwana-Kondoo,[n] lakini, kwa sababu yeye ni Bwana wa mabwana
na Mfalme wa wafalme,[o] Mwana-Kondoo atawashinda.[p] Pia, wale
walioitwa na waliochaguliwa na
walio waaminifu pamoja naye
watawashinda."[q]

15 Naye ananiambia: "Yale
maji uliyoyaona, ambapo yule

SURA 17

a Ufu 20:1
b Kut 32:32
Zb 69:28
Flp 4:3
c Ufu 13:8
d Mt 24:15
Yak 3:17
e Ufu 17:7
f Yer 51:25
g Yer 46:2
Yer 51:11
Da 8:20
Da 8:21
Sef 2:13
h Yoh 19:15
i Da 8:23
j Ufu 13:11
Ufu 19:20
k Ufu 17:8
l Da 7:24
m Zb 2:2
n Yoh 1:29
Ufu 5:6
o Mt 28:18
Mdo 2:36
1Ti 6:15
p Ufu 19:15
q Ro 16:20

Safu ya 2

a Isa 57:20
Yer 51:13
b Da 7:24
Ufu 17:12
c Ufu 17:8
d Ufu 17:7
e Mwa 38:24
Law 21:9
Ufu 18:8
f Yos 11:20
Met 21:1
Yer 51:12
g Ufu 17:12
h Isa 55:11
i Ufu 17:5
j Isa 47:5

SURA 18

k Ufu 12:10
l Mt 17:2
Ufu 1:16
m Yer 50:2
n Isa 21:9
Yer 51:8
Ufu 14:8
o Zb 39:5
p Isa 13:21
Yer 50:39
Yer 51:37
q Yer 51:7
r Isa 47:5
Ufu 17:2
s Isa 23:8
t Met 19:10
Isa 47:1

kahaba anaketi, yanamaanisha
vikundi vya watu na umati na
mataifa na lugha.[a] **16** Na zile
pembe kumi[b] ulizoona, na yule
mnyama-mwitu,[c] hawa watamchukia yule kahaba[d] na kumfanya kuwa ukiwa na uchi,
nao watakula sehemu zake zenye nyama na kumteketeza kabisa kwa moto.[e] **17** Kwa maana Mungu alitia hilo ndani ya
mioyo yao ili kutekeleza wazo
lake,[f] kutekeleza lile wazo lao
moja kwa kumpa yule mnyama-mwitu ufalme wao,[g] mpaka maneno ya Mungu yatakapokwisha kutimizwa.[h] **18** Na
yule mwanamke[i] uliyemwona
anamaanisha lile jiji kubwa lililo na ufalme juu ya wafalme wa
dunia."[j]

18 Baada ya mambo haya nikamwona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka[k] kubwa; na dunia ikaangazwa nuru
kutokana na utukufu wake.[l]
2 Naye akapaaza kilio kwa
sauti yenye nguvu,[m] akisema:
"Ameanguka! Babiloni Mkubwa ameanguka,[n] naye amekuwa makao ya roho waovu na
mahali pa kuvizia pa kila pumzi[o] chafu na mahali pa kuvizia pa kila ndege mchafu na
mwenye kuchukiwa![p] **3** Kwa
kuwa mataifa yote yameanguka yakiwa majeruhi kwa sababu ya divai ya hasira ya uasherati wake,[q] na wafalme wa dunia walifanya uasherati[r] naye,
na wanabiashara[s] wa dunia wanaosafiri walikuwa matajiri
kutokana na nguvu za anasa
yake isiyo na aibu."[t]

4 Nami nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni ikise-

ma: "Tokeni kwake, watu wangu,[a] ikiwa hamtaki kushiriki
pamoja naye dhambi zake,[b] na ikiwa hamtaki kupokea sehemu ya mapigo yake. **5** Kwa
maana dhambi zake zimekusanyika pamoja mpaka mbinguni,[c] naye Mungu amekumbuka
matendo yake yasiyo ya haki.[d] **6** Mlipeni sawa na vile yeye
mwenyewe alivyolipa,[e] na mtendeeni mara mbili ya hivyo, ndiyo, mara mbili ya hesabu ya
mambo aliyoyatenda;[f] katika kikombe[g] ambacho ndani yake
alitia mchanganyiko mtilieni[h] mchanganyiko mara mbili[i] ya
hivyo. **7** Kwa kadiri alivyojitukuza mwenyewe na kuishi
katika anasa isiyo na aibu, kwa kadiri hiyo mpeni mateso na
maombolezo.[j] Kwa maana moyoni mwake anaendelea kusema, 'Ninaketi nikiwa malkia,[k] nami si mjane,[l] nami
sitaona maombolezo kamwe.'[m] **8** Hiyo ndiyo sababu katika
siku moja mapigo[n] yake yatakuja, kifo na kuomboleza na
njaa, naye atateketezwa kabisa kwa moto,[o] kwa sababu Yehova Mungu, aliyemhukumu, ni
mwenye nguvu.[p]

9 "Na wafalme[q] wa dunia waliofanya uasherati pamoja naye
na kuishi katika anasa isiyo na aibu watalia na kujipigapiga wenyewe kwa huzuni juu
yake,[r] wanapoutazama moshi[s] kutokana na kuungua kwake, **10** huku wao wakisimama
mbali kwa sababu ya woga wao wa kuteseka kwake na kusema,[t] 'Ole, ole, wewe jiji kubwa,[u] Babiloni wewe jiji lenye nguvu, kwa sababu katika saa moja hukumu yako imefika!'[v]

SURA 18

a Isa 48:20
Isa 52:11
Yer 50:8
Yer 51:45
Zek 2:7
b Yer 51:6
2Ko 6:17
c Yer 51:9
1Ti 5:24
d Yer 51:49
Yer 51:56
Ufu 16:19
e 2Th 1:6
f Zb 137:8
Yer 50:15
Yer 51:24
g Zb 75:8
Yer 51:7
Ufu 16:19
h Ufu 14:10
i Yer 17:18
Yer 50:21
j Yer 50:29
k Ufu 17:15
l Isa 47:8
m Zb 10:6
n Yer 50:13
o Law 21:9
Yer 51:58
Ebr 12:29
p Yer 50:34
q Isa 23:17
r Yer 50:46
Eze 27:35
s Ufu 18:18
t Eze 26:17
u Da 4:30
v Yer 51:8

Safu ya 2

a Eze 27:36
b Eze 27:30
c Eze 27:12
d Eze 27:22
e Eze 27:13
f 1Ti 6:10
g Mhu 5:10
h Eze 27:36
i Eze 27:30
j Eze 27:31
k Ufu 17:4
l Met 11:4
m Isa 23:14

11 "Pia, wanabiashara[a] wa dunia wanaosafiri wanalia na
kuomboleza juu yake,[b] kwa sababu hakuna yeyote wa kununua tena mali zao zilizojaa,
12 mali zilizojaa[c] za dhahabu na fedha na jiwe la thamani na
lulu na kitani bora na zambarau na hariri na vitambaa vyekundu; na kila kitu cha miti
iliyotiwa manukato na kila namna ya kitu cha pembe ya tembo na kila namna ya kitu kinachotokana na miti ya thamani
zaidi na cha shaba na cha chuma na cha marumaru;[d] **13** pia
mdalasini na kiungo cha Kihindi na uvumba na mafuta yenye marashi na ubani na divai
na mafuta ya zeituni na unga laini na ngano na ng'ombe na kondoo, na farasi na magari na watumwa na nafsi za binadamu.[e]
14 Ndiyo, tunda zuri ambalo nafsi yako ilitamani[f] limeondoka kwako, na vitu vyote vitamu
na vitu vyenye fahari vimeangamia kutoka kwako, na watu
hawatavipata tena kamwe.[g]

15 "Wanabiashara[h] wanaosafiri wa vitu hivyo, waliopata utajiri kutokana naye, wa-
tasimama mbali kwa sababu ya woga wao juu ya kuteseka kwake na kulia na kuomboleza,[i] **16** wakisema, 'Ole, ole
—lile jiji kubwa,[j] lililovikwa kitani bora na zambarau na
kitambaa chekundu, na kupambwa kitajiri kwa mapambo ya dhahabu na mawe ya thamani na lulu,[k] **17** kwa sababu katika saa moja mali nyingi hivyo
zimefanywa ukiwa!'[l]

"Na kila kapteni wa meli na kila mtu ambaye husafiri baharini mahali popote,[m] na mabaharia na wale wote ambao

hupata riziki baharini, wali-
simama mbali[a] **18** na kupaa-
za kilio walipokuwa wakiutaza-
ma moshi uliotokana na kute-
ketezwa kwake na kusema, ‘Ni
jiji gani lililo kama lile jiji ku-
bwa?’[b] **19** Nao wakatupa ma-
vumbi juu ya vichwa[c] vyao na
kupaaza kilio, wakilia na kuo-
mboleza,[d] na kusema, ‘Ole, ole,
—lile jiji kubwa, ambalo wale
wote walio na mashua bahari-
ni[e] walikuwa matajiri[f] kwa sa-
babu ya utajiri wake mkubwa,
kwa sababu katika saa moja
amefanywa ukiwa!’[g]
20 “Furahini juu yake, enyi
mbingu,[h] pia ninyi watakatifu[i]
na ninyi mitume[j] na ninyi ma-
nabii, kwa sababu Mungu ame-
mtoza adhabu ya hukumu kwa
ajili yenu!”[k]
21 Na malaika mwenye ngu-
vu akainua jiwe kama jiwe ku-
bwa la kusagia[l] na kulitupa nda-
ni ya bahari,[m] akisema: “Hivi
ndivyo Babiloni lile jiji kubwa
litakavyotupwa chini kwa mtu-
po wa kasi sana, naye hatapati-
kana tena.[n] **22** Na sauti ya
waimbaji ambao hufuatanisha
sauti zao kwa kinubi na ya wa-
namuziki na ya wapiga-filimbi
na ya wapiga-tarumbeta haita-
sikiwa tena kamwe ndani yako,[o]
na hakuna fundi wa kazi yo-
yote atakayepatikana ndani
yako tena kamwe, na hakuna
sauti ya jiwe la kusagia ita-
kayosikiwa tena kamwe ndani
yako, **23** na hakuna nuru ya
taa itakayoangaza tena kamwe
ndani yako, na hakuna sau-
ti ya bwana-arusi na bibi-arusi
itakayosikiwa tena kamwe nda-
ni yako;[p] kwa sababu wanabi-
ashara[q] wako wanaosafiri wa-
likuwa ndio watu wenye dara-
ja la juu[a] wa dunia, kwa ma-
ana mataifa yote yalipotoshwa
kwa mazoea yako ya kuwasili-
ana na pepo.[b] **24** Ndiyo, nda-
ni yake ilipatikana damu[c] ya
manabii[d] na ya watakatifu[e] na
ya wale wote ambao wameu-
awa juu ya dunia.”[f]
19 Baada ya mambo haya
nikasikia kitu kama sa-
uti kubwa ya umati mkubwa
mbinguni.[g] Walisema: “Msifu-
ni Yah![h] Wokovu[i] na utukufu
na nguvu ni za Mungu wetu,[j]
2 kwa sababu hukumu zake ni
za kweli na za uadilifu.[k] Kwa
maana ametekeleza hukumu
juu ya yule kahaba mkubwa ali-
yeiharibu dunia kwa uasheri-
ati wake, naye amelipiza ki-
sasi damu ya watumwa wake
mkononi mwake.”[l] **3** Na mara
moja, kwa mara ya pili waka-
sema:[m] “Msifuni Yah! Na moshi
kutoka kwake unaendelea ku-
panda milele na milele.”[n]
4 Na wale wazee 24[o] na wale
viumbe hai wanne[p] wakaangu-
ka chini na kumwabudu Mungu
anayeketi[q] juu ya kiti cha ufa-
lme, na kusema: “Amina! Msifu-
ni Yah!”[r]
5 Pia, sauti ikatoka katika
kile kiti cha ufalme na kusema:
“Muwe mkimsifu Mungu wetu,
enyi nyote watumwa wake,[s]
ambao mnamwogopa, wadogo
kwa wakubwa.”[t]
6 Nami nikasikia kitu kama
sauti ya umati mkubwa na
kama sauti ya maji mengi na
kama sauti ya ngurumo nzito.
Wakasema: “Msifuni Yah,[u] kwa
sababu Yehova Mungu wetu,
Mweza-Yote,[v] ameanza kuta-
wala akiwa mfalme.[w] **7** Ache-
ni tushangilie na kuwa wenye

SURA 18

a Eze 27:27
b Eze 27:32
c 1Sa 4:12
d Eze 27:30
e Eze 27:9
f Eze 27:33
g Isa 47:11
Yer 51:55
h Yer 51:48
Ufu 12:12
i Ufu 14:12
j 1Ko 4:9
k Kum 32:43
Ro 12:19
Ufu 6:10
Ufu 19:2
l Mt 18:6
m Yer 51:63
n Yer 51:64
Eze 26:21
o Isa 24:8
Eze 26:13
p Yer 25:10
q Isa 23:8

Safu ya 2

a Mk 6:21
b Isa 47:9
Ga 5:20
Ufu 9:21
c Ufu 6:10
d Mt 23:37
e Ufu 16:6
f Mwa 9:6
Yer 51:49

SURA 19

g Da 7:10
h Zb 150:6
i Ufu 12:10
j Ufu 7:12
k Kum 32:4
Zb 19:9
1Pe 1:17
Ufu 15:3
l Kum 32:43
2Fa 9:7
Zb 79:10
Ufu 18:20
Ufu 18:24
m Zb 117:1
n Isa 34:10
o Ufu 4:4
p Ufu 4:6
q 1Fa 22:19
Isa 6:1
r Zb 106:48
s Zb 134:1
Zb 135:1
t Zb 115:13
u Zb 113:1
v Kut 6:3
w Zb 97:1
Isa 52:7
Da 7:9
Ufu 11:15

shangwe mno, na tumpe yeye
utukufu,[a] kwa sababu ndoa[b]
ya Mwana-Kondoo imefika[c] na
mke wake amejitayarisha.[d]
8 Ndiyo, amepewa ruhusa ya
kupambwa kitani bora, changa-
vu, safi, kwa maana hicho ki-
tani bora humaanisha matendo
ya uadilifu ya watakatifu."[e]

9 Naye ananiambia: "Andi-
ka: Wenye furaha ni wale walio-
alikwa[f] kwenye mlo wa jioni wa
ndoa ya Mwana-Kondoo."[g] Pia,
ananiambia: "Hayo ndiyo mane-
no ya kweli ya Mungu."[h]
10 Ndipo nikaanguka chini
mbele ya miguu yake ili kumwa-
budu yeye.[i] Lakini yeye ana-
niambia: "Uwe mwangalifu! Usi-
fanye hivyo![j] Mimi ni mtumwa
mwenzako tu na wa ndugu zako
walio na kazi ya kutoa ushahidi
kumhusu Yesu.[k] Mwabudu Mu-
ngu;[l] kwa maana kutoa ushahi-
di kumhusu Yesu ndilo kusudi
la unabii."[m]

11 Nami nikaona mbingu
imefunguliwa, na, tazama! fa-
rasi mweupe.[n] Na yeye aliyeke-
ti juu yake anaitwa Mwamini-
fu[o] na wa Kweli,[p] naye anahu-
kumu na kufanya vita kwa ua-
dilifu.[q] **12** Macho yake ni
mwali wa moto,[r] na juu ya ki-
chwa chake kuna vilemba vi-
ngi.[s] Ana jina[t] lililoandikwa
ambalo hakuna yeyote anaye-
lijua isipokuwa yeye mwenye-
we, **13** naye amepambwa vazi
la nje lililonyunyiziwa damu,[u]
na jina analoitwa ni Neno la
Mungu.[v] **14** Pia, majeshi yali-
yokuwa mbinguni yalikuwa ya-
kimfuata juu ya farasi weupe,
nayo yalikuwa yamevikwa ki-
tani bora cheupe, safi. **15** Na
upanga mrefu mkali unacho-
moza kutoka kinywani mwa-

SURA 19

a Ufu 7:12
b Mt 25:10
Ufu 19:9
c 1Th 4:16
d 2Ko 11:2
e Isa 61:10
Efe 5:27
Ufu 14:4
f Mt 22:3
Lu 14:17
g Lu 14:15
h Yoh 3:34
Yoh 8:47
i Ufu 22:8
j Mdo 10:26
Ufu 22:9
k Mt 28:19
Mdo 1:8
l Mt 4:10
Yoh 4:23
m Lu 24:27
Mdo 2:17
Mdo 10:43
1Pe 1:11
n Ayu 39:25
Met 21:31
Yer 8:6
Ufu 6:2
o Ebr 3:6
Ufu 1:5
p Yoh 1:14
Ufu 3:14
q Isa 11:4
Ebr 1:8
Ebr 1:9
r Ufu 1:14
Ufu 2:18
s Ufu 19:16
t Ufu 2:17
u Ebr 12:24
1Pe 1:2
v Yoh 1:1
1Yo 1:1

Safu ya 2

a 2Th 2:8
Ufu 1:16
b Zb 2:9
Ufu 2:27
Ufu 12:5
c Yer 25:30
Yoe 3:13
Ufu 14:20
d Ufu 14:19
e Mt 28:18
Flp 2:10
1Ti 6:15
Ufu 17:14
f 1Sa 17:46
Eze 39:4
Eze 39:17
g Eze 39:17
h Eze 39:18
i Eze 39:20
j Ufu 13:1
k Ufu 16:14
Ufu 17:12
l Eze 38:16
Ufu 16:16
m Zb 2:2
n Ufu 13:18
o Ufu 13:11
Ufu 16:13
p Ufu 13:13
q Ufu 13:16
r Ufu 13:15
s Mt 10:28
2Pe 2:6
Yud 7
Ufu 20:14
t Ufu 6:2

ke,[a] ili ayapige mataifa nao,
naye atawachunga kwa fimbo
ya chuma.[b] Yeye anakanyaga
pia shinikizo la divai[c] ya hasira
ya ghadhabu ya Mungu[d] Mwe-
za-Yote. **16** Na juu ya vazi
lake la nje, juu ya paja lake, ana
jina ambalo limeandikwa, Mfa-
lme wa wafalme na Bwana wa
mabwana.[e]

17 Nikaona pia malaika ame-
simama katika jua, naye akap-
aaza kilio kwa sauti kubwa na
kuwaambia ndege[f] wote wanao-
ruka katikati ya mbingu: "Njo-
oni hapa, mkusanyike pamoja
kwenye mlo mkubwa wa jioni
wa Mungu, **18** ili mpate kula
sehemu zenye nyama za wafa-
lme na sehemu zenye nyama[g]
za viongozi wa kijeshi na sehe-
mu zenye nyama za watu wenye
nguvu[h] na sehemu zenye nya-
ma za farasi[i] na za wale wanao-
keti juu yao, na sehemu zenye
nyama za wote, za watu huru
na vilevile za watumwa na za
wadogo na wakubwa."

19 Nami nikamwona yule
mnyama-mwitu[j] na wafalme[k]
wa dunia na majeshi yao wame-
kusanyika pamoja ili kupiga-
na vita[l] na yule anayeketi juu
ya farasi[m] na jeshi lake. **20** Na
yule mnyama-mwitu[n] akaka-
matwa, na yule nabii wa uwo-
ngo[o] pamoja naye, aliyefanya
mbele yake ishara[p] alizotumia
kuwapotosha wale waliopokea
alama[q] ya yule mnyama-mwi-
tu na wale wanaoitolea sana-
mu[r] yake ibada. Wakiwa bado
hai, wote wawili walitupwa nda-
ni ya ziwa la moto linalowaka
kwa kiberiti.[s] **21** Lakini wale
wengine wakauawa kabisa kwa
ule upanga mrefu wa yule ana-
yeketi juu ya farasi,[t] upanga

uliochomoza kinywani mwake.[a]
Na ndege[b] wote wakashiba[c] se-
hemu zao zenye nyama.[d]

20 Nami nikamwona malai-
ka akishuka kutoka mbi-
nguni mwenye ufunguo wa abi-
so[e] na mnyororo mkubwa mko-
noni mwake. **2** Naye akamka-
mata yule joka[f] mkubwa, yule
nyoka wa zamani,[g] ambaye ni
Ibilisi[h] na Shetani,[i] na kumfu-
nga kwa miaka elfu. **3** Naye
akamtupa ndani ya abiso[j] na
kuifunga na kuitia muhuri juu
yake, ili asipotoshe mataifa
tena mpaka ile miaka elfu ita-
kapokwisha. Baada ya mambo
hayo yeye atafunguliwa kwa
muda kidogo.[k]

4 Nami nikaona viti vya ufa-
lme,[l] na kulikuwa na wale wali-
oketi juu yake, nao wakapewa
mamlaka ya kuhukumu.[m] Ndi-
yo, niliona nafsi za wale wa-
liouawa kwa shoka kwa aji-
li ya ushahidi waliotoa kumhu-
su Yesu na kwa ajili ya kusema
juu ya Mungu, na wale ambao
hawakumwabudu yule mnya-
ma-mwitu[n] wala sanamu[o] yake
na ambao hawakupokea ile ala-
ma juu ya paji la uso wao na
juu ya mkono wao.[p] Nao wa-
kawa hai na kutawala waki-
wa wafalme[q] pamoja na Kri-
sto kwa miaka elfu. **5** (Wale
wafu[r] wengine hawakuwa hai
mpaka ile miaka elfu ilipokwi-
sha.)[s] Huo ndio ufufuo wa
kwanza.[t] **6** Mwenye furaha[u]
na mtakatifu[v] ni yeyote aliye
na sehemu katika ufufuo wa
kwanza; kifo cha pili[w] hakina
mamlaka juu ya hao,[x] bali wa-
takuwa makuhani[y] wa Mungu
na wa Kristo, nao watatawala
wakiwa wafalme pamoja naye
ile miaka elfu.[z]

SURA 19

a Ufu 2:16
b Eze 39:4
Ufu 19:17
c Eze 39:20
d Eze 39:17

SURA 20

e Ufu 9:1
f Ufu 12:3
g Mwa 3:1
h Yoh 8:44
i Zek 3:1
Ufu 12:9
j Ufu 9:11
k Ufu 20:7
l Lu 22:30
m Mt 19:28
Lu 22:30
1Ko 6:2
n Ufu 13:12
o Ufu 13:15
p Ufu 13:16
q 2Ti 2:12
Ufu 1:6
r Yoh 5:28
Mdo 24:15
Efe 2:1
s Mt 25:46
Ufu 20:13
t 1Ko 15:23
1Ko 15:52
Flp 3:11
1Th 4:16
u Ufu 14:13
Ufu 22:7
v Ufu 13:10
w Mt 10:28
Ufu 2:11
Ufu 20:14
x 1Ko 15:54
y 1Pe 2:9
Ufu 1:6
z Ufu 5:10

Safu ya 2

a Eze 38:15
b Eze 48:35
Ufu 21:3
c Ebr 12:22
Ufu 21:2
d 2Fa 1:10
Eze 38:22
e Ufu 12:9
f Ufu 13:1
g Ufu 19:20
h Ebr 12:23
Ufu 4:2
i 2Pe 3:7
j Mdo 24:15
Ufu 11:18
k Kut 32:33
Zb 69:28
Da 12:1
l Yoh 5:29
m Mdo 10:42
n Yoh 5:29
o Isa 25:8
Ro 5:12
1Ko 15:26

7 Sasa mara tu ile miaka elfu
itakapokwisha, Shetani atafu-
nguliwa kutoka katika gereza
lake, **8** naye ataenda kuyapo-
tosha yale mataifa yaliyo kati-
ka pembe nne za dunia, Gogu
na Magogu, kuwakusanya pa-
moja kwa ajili ya vita. Hesabu
yao ni kama mchanga wa bahari.[a]
9 Nao wakasonga juu ya
upana wa dunia na kuizungu-
ka kambi ya watakatifu[b] na lile
jiji[c] linalopendwa. Lakini moto
ukashuka kutoka mbinguni na
kuwateketeza.[d] **10** Na Ibilisi[e]
aliyekuwa akiwapotosha alitu-
pwa ndani ya lile ziwa la moto
na kiberiti, ambamo wote wawi-
li, yule mnyama-mwitu[f] na yule
nabii wa uwongo, tayari wali-
kuwa;[g] nao watateswa mchana
na usiku milele na milele.

11 Nami nikaona kiti cha
ufalme kikubwa cheupe na
yeye aliyeketi juu yake.[h] Du-
nia na mbingu zikakimbia ku-
toka mbele zake,[i] na maha-
li popote hapakupatikana kwa
ajili ya hizo. **12** Nami nikawa-
ona wafu, wakubwa kwa wado-
go,[j] wamesimama mbele ya kile
kiti cha ufalme, na vitabu vya
kukunjwa vikafunguliwa. La-
kini kitabu kingine cha kuku-
njwa kikafunguliwa; hicho ni
kitabu cha uzima.[k] Na wafu
wakahukumiwa kutokana na
mambo yale yaliyoandikwa kati-
ka vile vitabu kulingana na ma-
tendo yao.[l] **13** Na bahari ika-
watoa wale wafu waliokuwa
ndani yake, na kifo na Kabu-
ri* vikawatoa wale wafu[m] wali-
okuwa ndani yake, nao walihu-
kumiwa kila mmoja kulingana
na matendo yake.[n] **14** Na kifo[o]

Ufu 20:13* Hadesi. Tazama Nyongeza 4.

na Kaburi* vikatupwa ndani ya
lile ziwa la moto. Hili linamaa-
nisha kifo cha pili,[a] lile ziwa la
moto.[b] **15** Zaidi ya hayo, yeyo-
te ambaye hakupatikana amea-
ndikwa katika kile kitabu cha
uzima[c] alitupwa ndani ya lile
ziwa la moto.[d]

21 Nami nikaona mbingu
mpya[e] na dunia mpya;[f]
kwa maana mbingu[g] ya kwa-
nza na dunia[h] ya kwanza zi-
likuwa zimepitilia mbali, na
bahari[i] haipo tena. **2** Nikao-
na pia lile jiji takatifu,[j] Yeru-
salemu Jipya, likishuka kutoka
mbinguni[k] kwa Mungu na lime-
tayarishwa kama bibi-arusi[l] aliy-
epambwa kwa ajili ya mume
wake.[m] **3** Ndipo nikasikia sa-
uti kubwa kutoka katika kile
kiti cha ufalme ikisema: "Ta-
zama! Hema[n] la Mungu liko
pamoja na wanadamu, naye
atakaa[o] pamoja nao, nao wata-
kuwa watu wake.[p] Na Mungu
mwenyewe atakuwa pamoja
nao.[q] **4** Naye atafuta kila cho-
zi[r] kutoka katika macho yao,
na kifo hakitakuwapo tena,[s]
wala maombolezo wala kilio
wala maumivu hayatakuwapo
tena.[t] Mambo ya zamani yame-
pitilia mbali."[u]

5 Na Yule aliyeketi juu ya
kiti cha ufalme[v] akasema: "Ta-
zama! Ninafanya vitu vyote
kuwa vipya."[w] Pia, anasema:
"Andika, kwa sababu maneno
haya ni ya uaminifu na ya kwe-
li." **6** Naye akaniambia: "Ya-
mekuwa! Mimi ndiye Alfa na
Omega, mwanzo na mwisho.[x]
Kwa yeyote aliye na kiu mimi
nitampa maji bure kutoka kwe-
nye chemchemi ya maji ya uzi-
ma.[a] **7** Yeyote anayeshinda
atarithi vitu hivi, nami nita-
kuwa Mungu wake[b] naye ata-
kuwa mwanangu.[c] **8** Lakini
kwa habari ya waoga na wale
wasio na imani[d] na wale we-
nye kuchukiza katika uchafu[e]
wao na wauaji[f] na waasherati[g]
na wale wanaozoea kuwasiliana
na pepo na waabudu-sanamu[h]
na waongo[i] wote, fungu lao lita-
kuwa ndani ya lile ziwa linalo-
waka moto[j] na kiberiti.[k] Hili li-
namaanisha kifo cha pili."[l]

9 Na akaja mmoja wa wale
malaika saba waliokuwa na ma-
bakuli saba yaliyojaa mapigo
saba ya mwisho,[m] naye akase-
ma nami na kuniambia: "Njoo
hapa, nitakuonyesha bibi-arusi,
mke wa Mwana-Kondoo."[n]
10 Kwa hiyo akanichukua kati-
ka nguvu za roho mpaka kwe-
nye mlima mkubwa na mrefu
sana,[o] naye akanionyesha lile
jiji takatifu[p] Yerusalemu liki-
shuka kutoka mbinguni kwa
Mungu[q] **11** na likiwa na utu-
kufu wa Mungu.[r] Mwangaza
wake ulikuwa kama jiwe la tha-
mani zaidi, kama jiwe la ya-
spi lenye kung'aa kwa uangavu
kama fuwele.[s] **12** Lilikuwa na
ukuta[t] mkubwa na mrefu sana
nalo lilikuwa na malango kumi
na mawili, na kwenye hayo ma-
lango malaika kumi na wawili,
na majina yalikuwa yameandi-
kwa ambayo ni yale ya makabi-
la kumi na mawili ya wana wa
Israeli.[u] **13** Upande wa ma-
shariki kulikuwa na malango
matatu, na upande wa kaskazi-
ni malango matatu, na upa-
nde wa kusini malango mata-
tu, na upande wa magharibi

SURA 20
a Ufu 2:11
Ufu 20:6
Ufu 21:8
b Mt 5:22
Mt 18:9
Yak 3:6
c Ufu 17:8
d Met 10:7
Ufu 21:8

SURA 21
e Isa 65:17
2Pe 3:13
f Isa 66:22
g 2Pe 3:10
h Ufu 20:11
i Isa 57:20
Ufu 17:15
j Isa 52:1
k Ebr 12:22
Ufu 3:12
l Ufu 19:7
m Mt 9:15
Yoh 3:29
n Eze 37:27
o Zb 15:1
p Isa 66:23
q Eze 43:7
Eze 48:35
r Isa 65:19
Ufu 7:17
s Isa 25:8
1Ko 15:26
t Isa 35:10
Isa 65:19
u 2Pe 3:7
v 2Nya 18:18
Isa 6:1
Ufu 4:2
w Isa 42:9
Omb 5:21
Eze 36:26
2Pe 3:13
x Ufu 1:8
Ufu 22:13

Safu ya 2
a Zb 36:9
Isa 55:1
Ufu 7:17
Ufu 22:1
b 1Ko 15:28
Ufu 3:12
c 2Sa 7:14
d Ro 11:20
Ebr 3:19
1Yo 5:10
e Ro 1:24
1Ko 6:9
f 1Yo 3:15
g Efe 5:5
h Ga 5:20
i Yoh 8:44
Mdo 5:3
1Ti 1:10
j Mt 5:22
Mt 18:9
Yak 3:6
k Isa 30:33
Mt 10:28
Ufu 19:20
l Met 10:7
Ebr 10:26
Ufu 2:11
Ufu 20:6
m Law 26:21
Ufu 15:1
n Zb 45:9
Ufu 19:7
o Isa 2:2
Eze 40:2
Mik 4:1
p Isa 52:1

Ufu 20:14* Hadesi. Tazama Nyongeza 4.

q Ebr 12:22; Ufu 3:12; Ufu 21:2; r Isa 60:1; s Kut 24:10; t Isa 60:18; u Kut 28:21; Kut 39:14.

malango matatu.[a] **14** Ukuta wa jiji lile pia ulikuwa na mawe ya msingi[b] kumi na mawili, na juu ya hayo majina kumi na mawili ya mitume[c] kumi na wawili wa Mwana-Kondoo.

15 Basi yeye aliyekuwa akisema nami alikuwa ameshika utete wa dhahabu kuwa kipimio,[d] ili alipime jiji lile na malango yake na ukuta wake.[e] **16** Na jiji linakaa mraba, na urefu wake ni mkubwa kama upana wake. Naye akalipima jiji[f] kwa utete, stadia elfu kumi na mbili; urefu wake na upana wake na kimo chake ni sawa. **17** Pia, akapima ukuta wake, mikono 144, kulingana na kipimo cha mwanadamu, na wakati huohuo cha malaika. **18** Basi muundo wa ukuta wake ulikuwa yaspi,[g] na jiji lilikuwa dhahabu safi kama kioo safi. **19** Misingi[h] ya ukuta wa jiji ilikuwa imepambwa kwa kila namna ya jiwe la thamani:[i] msingi wa kwanza ulikuwa yaspi,[j] wa pili yakuti,[k] wa tatu kalkedoni, wa nne zumaridi,[l] **20** wa tano sardoniksi, wa sita sardio, wa saba krisolito,[m] wa nane beroli, wa tisa topazi,[n] wa kumi krisopraso, wa kumi na moja hayasinthi, wa kumi na mbili amethisto.[o] **21** Pia, yale malango kumi na mawili yalikuwa lulu kumi na mbili; kila moja la malango lilifanyizwa kwa lulu moja.[p] Na njia pana ya jiji ilikuwa dhahabu safi, kama kioo kiangavu.

22 Nami sikuona hekalu ndani yake,[q] kwa maana Yehova[r] Mungu Mweza-Yote[s] ndiye hekalu lake,[t] na pia Mwana-Kondoo.[u] **23** Na jiji lile halihitaji jua wala mwezi kuliangaza,

SURA 21

a Ufu 22:14
b Ebr 11:10
c Mt 10:2
Lu 6:13
Mdo 1:13
Efe 2:20
d Eze 40:3
Ufu 11:1
e Eze 40:5
f Ufu 3:12
g Ufu 4:3
Ufu 21:11
h Isa 54:11
i Isa 54:12
j Kut 28:18
Eze 28:13
k Kut 39:11
Ayu 28:6
l Kut 28:17
Ufu 4:3
m Kut 28:20
Wim 5:14
Eze 1:16
Da 10:6
n Kut 28:17
Kut 39:10
Ayu 28:19
Eze 28:13
o Kut 28:19
Kut 39:12
p Est 1:6
Ayu 28:18
Mt 13:46
q Mdo 7:49
r Zb 11:4
s Kut 6:3
Ufu 15:3
t Yoh 4:23
u Efe 2:20

Safu ya 2

a Isa 60:19
Ufu 22:5
b Yoh 1:9
Mdo 26:13
Ebr 1:3
c Isa 60:3
d Zb 138:4
e Isa 60:11
f Isa 60:20
g Isa 60:5
h 1Ko 6:9
Ga 5:21
i Zb 5:6
Kol 3:9
Ufu 21:8
j Isa 52:1
k Da 12:1
Flp 4:3
Ufu 13:8

SURA 22

l Eze 47:1
m Yoh 1:29
n Ufu 2:7
o Eze 47:12
p Eze 47:12
q Zek 14:11
r Zb 9:7
s Ufu 3:21
t Ro 1:9
u Zb 17:15
Mt 5:8
v Ufu 14:1
w Ufu 21:25

kwa maana utukufu wa Mungu ulilitia nuru,[a] na taa yake ilikuwa yule Mwana-Kondoo.[b] **24** Na mataifa yatatembea kwa njia ya nuru yake,[c] na wafalme wa dunia wataleta utukufu wao ndani yake.[d] **25** Na malango yake hayatafungwa hata kidogo wakati wa mchana,[e] kwa maana usiku hautakuwa humo.[f] **26** Nao wataleta utukufu na heshima ya mataifa ndani yake.[g] **27** Lakini kitu chochote kisicho kitakatifu na yeyote anayeendelea kutenda chukizo[h] na uwongo[i] hataingia ndani yake hata kidogo;[j] watakaoingia ni wale tu walioandikwa katika kile kitabu cha kukunjwa cha uzima cha Mwana-Kondoo.[k]

22 Naye akanionyesha mto wa maji ya uzima,[l] mwangavu kama fuwele, ukitiririka kutoka katika kiti cha ufalme cha Mungu na cha Mwana-Kondoo[m] **2** ukiteremka kupitia katikati ya njia yake pana. Na upande huu wa mto na upande ule kulikuwa na miti[n] ya uzima yenye kuzaa mazao kumi na mawili ya matunda, ikitoa matunda yake kila mwezi.[o] Na majani ya miti ile yalikuwa ya kuponya mataifa.[p]

3 Na humo haitakuwapo laana yoyote tena.[q] Bali kiti cha ufalme cha Mungu[r] na cha Mwana-Kondoo[s] kitakuwa katika jiji hilo, na watumwa wake watamtolea utumishi mtakatifu;[t] **4** nao watauona uso wake,[u] na jina lake litakuwa juu ya mapaji ya nyuso zao.[v] **5** Pia, usiku hautakuwapo tena,[w] na hawana uhitaji wa nuru ya taa wala hawana nuru ya jua, kwa sababu Yehova Mungu ata-

angaza nuru[a] yake juu yao, nao
watatawala wakiwa wafalme mi-
lele na milele.[b]
6 Naye akaniambia: "Maneno haya ni ya uaminifu na ya
kweli;[c] ndiyo, Yehova Mungu
wa maneno ya manabii yaliyoongozwa na roho[d] alimtuma malaika wake ili kuwaonyesha watumwa wake mambo ambayo lazima yatendeke upesi.[e] **7** Na,
tazama! mimi ninakuja upesi.[f]
Mwenye furaha ni yeyote anayeshika maneno ya unabii wa
kitabu hiki cha kukunjwa."[g]
8 Basi, mimi Yohana ndiye
niliyekuwa nikisikia na kuona mambo haya. Na nilipokuwa nimesikia na kuona, nikaanguka chini kuabudu[h] mbele ya miguu ya yule malaika aliyekuwa akinionyesha mambo haya. **9** Lakini yeye
akaniambia: "Uwe mwangalifu!
Usifanye hivyo! Mimi ni mtumwa mwenzako tu na wa ndugu zako walio manabii[i] na wa
wale wanaoshika maneno ya kitabu hiki cha kukunjwa. Mwabudu Mungu."[j]
10 Pia yeye akaniambia: "Usiyatie muhuri maneno ya unabii
wa kitabu hiki cha kukunjwa,
kwa maana wakati uliowekwa
uko karibu.[k] **11** Yeye anayetenda ukosefu wa uadilifu, na azidi kutenda ukosefu wa uadilifu;[l] na mwenye uchafu azidi
kufanywa mwenye uchafu;[m] lakini mwadilifu[n] na azidi kufanya uadilifu, na mtakatifu azidi
kufanywa kuwa mtakatifu.[o]
12 "'Tazama! Mimi ninakuja upesi,[p] na thawabu[q] ninayotoa ipo pamoja nami, ili kumlipa
kila mmoja kulingana na matendo yake.[r] **13** Mimi ndiye Alfa
na Omega,[s] wa kwanza na wa
mwisho,[a] mwanzo na mwisho.
14 Wenye furaha ni wale wanaofua kanzu zao,[b] ili wawe na
mamlaka ya kwenda kwenye
miti ya uzima[c] na kwamba waweze kuingia katika jiji kupitia
malango yake.[d] **15** Nje kuna
mbwa[e] na wale wenye mazoea ya kuwasiliana na pepo[f] na
waasherati[g] na wauaji na waabudu-sanamu na kila mtu anayependezwa na uwongo[h] na kuendelea kuutenda.'

16 "'Mimi, Yesu, nilimtuma
malaika wangu kuwatolea ninyi ushahidi juu ya mambo
haya kwa ajili ya yale makutaniko. Mimi ndiye mzizi[i] na uzao[j]
wa Daudi, na nyota nyangavu
ya asubuhi.'"[k]
17 Na roho[l] na bibi-arusi[m] huendelea kusema: "Njoo!"
Na yeyote anayesikia na aseme: "Njoo!"[n] Na yeyote anaye-
ona kiu aje;[o] yeyote anayetaka
achukue maji ya uzima bure.[p]
18 "Ninamtolea ushahidi
kila mtu anayesikia maneno ya
unabii wa kitabu hiki cha kukunjwa: Yeyote akiongeza[q] kwenye mambo haya, Mungu ata-
mwongezea mapigo[r] yaliyoandikwa katika kitabu hiki; **19** na
yeyote akiondoa lolote kutoka
katika maneno ya kitabu cha
unabii huu, Mungu ataondoa fungu lake kutoka katika ile miti
ya uzima[s] na kutoka katika lile
jiji takatifu,[t] mambo ambayo yameandikwa katika kitabu hiki
cha kukunjwa.
20 "Yeye anayetoa ushahidi
juu ya mambo haya asema, 'Ndiyo; mimi ninakuja upesi.'"[u]
"Amina! Njoo, Bwana Yesu."
21 Fadhili zisizostahiliwa za
Bwana Yesu Kristo na ziwe pamoja na watakatifu.[v]

SURA 22

a Isa 60:19
1Yo 1:5
b Da 7:18
Ufu 3:21
Ufu 14:1
c Tit 1:2
Ufu 21:5
d 1Sa 3:21
2Sa 23:2
Yer 37:6
2Ti 3:16
e Ufu 1:1
f Ufu 16:15
Ufu 22:20
g Yoh 13:17
Ufu 1:3
h Mdo 10:25
i Yoe 2:28
j Zb 29:2
Mt 4:10
Ufu 19:10
k Ufu 1:3
l Da 12:10
m 2Ti 3:13
Yud 10
n Ro 5:1
o Flp 3:16
1Pe 1:15
p Isa 40:10
q Ebr 11:6
r Zb 62:12
Met 24:12
Yer 17:10
Ro 2:6
s Isa 44:6
Ufu 1:8
Ufu 21:6

Safu ya 2

a Isa 48:12
b 1Yo 1:7
Ufu 1:3
c Ufu 2:7
d Ufu 21:12
e Kum 23:18
Mt 7:6
Flp 3:2
f Ga 5:20
g Efe 5:5
h Kol 3:9
Ufu 21:8
i Isa 11:10
Ufu 5:5
j Isa 11:1
Isa 53:2
Yer 23:5
Yer 33:15
Ro 1:3
k Hes 24:17
Ufu 2:28
l Ufu 22:6
m Ufu 21:9
n Mt 11:28
o Yoh 4:14
p Isa 55:1
Yoh 7:37
Ufu 7:17
Ufu 21:6
q Kum 4:2
Kum 12:32
Met 30:6
Yoh 20:30
2Ko 11:4
Ga 1:8
1Yo 4:3
r 2Yo 9
Ufu 15:1
s Ufu 2:7
Ufu 22:2
t Ufu 21:2
u Ufu 3:11
Ufu 22:7
v Ro 16:20
2Th 3:18

ORODHA YA VITABU VYA BIBLIA

Vitabu vya Maandiko ya Kiebrania Kabla ya Wakati wa Kawaida (wa Ukristo)

Jina la Kitabu	Mwandikaji	Mahali Kilipoandikiwa	Uandikaji Ulikamilishwa (K.W.K.)	Muda Unaohusika (K.W.K.)
Mwanzo	Musa	Nyikani	1513	"Hapo mwanzo" mpaka 1657
Kutoka	Musa	Nyikani	1512	1657-1512
Mambo ya Walawi	Musa	Nyikani	1512	Mwezi 1 (1512)
Hesabu	Musa	Nyikani na Nchi Tambarare za Moabu	1473	1512-1473
Kumbukumbu la Torati	Musa	Nchi Tambarare za Moabu	1473	Miezi 2 (1473)
Yoshua	Yoshua	Kanaani	m. 1450	1473–m. 1450
Waamuzi	Samweli	Israeli	m. 1100	m. 1450–m. 1120
Ruthu	Samweli	Israeli	m. 1090	Miaka 11 ya utawala wa Waamuzi
1 Samweli	Samweli; Gadi; Nathani	Israeli	m. 1078	m. 1180-1078
2 Samweli	Gadi; Nathani	Israeli	m. 1040	1077–m. 1040
1 Wafalme	Yeremia	Yuda na	Kitabu 1	m. 1040-580
2 Wafalme	Yeremia	Misri	580	
1 Mambo ya Nyakati	Ezra	Yerusalemu (?)	Kitabu 1	Baada ya 1 Mambo ya Nyakati 9:44: 1077-537
2 Mambo ya Nyakati	Ezra	Yerusalemu (?)	m. 460	
Ezra	Ezra	Yerusalemu	m. 460	537–m. 467
Nehemia	Nehemia	Yerusalemu	b. 443	456–b. 443
Esta	Mordekai	Shushani, Elamu	m. 475	493–m. 475
Ayubu	Musa	Nyikani	m. 1473	Zaidi ya miaka 140 kati ya 1657 na 1473
Zaburi	Daudi na wengine		m. 460	
Methali	Sulemani; Aguri; Lemueli	Yerusalemu	m. 717	
Mhubiri	Sulemani	Yerusalemu	k. 1000	
Wimbo wa Sulemani	Sulemani	Yerusalemu	m. 1020	
Isaya	Isaya	Yerusalemu	b. 732	m. 778–b. 732
Yeremia	Yeremia	Yuda; Misri	580	647-580
Maombolezo	Yeremia	Karibu na Yerusalemu	607	
Ezekieli	Ezekieli	Babiloni	m. 591	613–m. 591
Danieli	Danieli	Babiloni	m. 536	618–m. 536
Hosea	Hosea	Samaria (Wilaya)	b. 745	k. 804–b. 745
Yoeli	Yoeli	Yuda	m. 820 (?)	
Amosi	Amosi	Yuda	m. 804	
Obadia	Obadia		m. 607	
Yona	Yona		m. 844	
Mika	Mika	Yuda	k. 717	m. 777-717
Nahumu	Nahumu	Yuda	k. 632	
Habakuki	Habakuki	Yuda	m. 628 (?)	
Sefania	Sefania	Yuda	k. 648	
Hagai	Hagai	Yerusalemu lililojengwa upya	520	Siku 112 (520)
Zekaria	Zekaria	Yerusalemu lililojengwa upya	518	520-518
Malaki	Malaki	Yerusalemu lililojengwa upya	b. 443	

Vitabu vya Maandiko ya Kigiriki Vilivyoandikwa Katika Wakati wa Kawaida (wa Ukristo)

Jina la Kitabu	Mwandikaji	Mahali Kilipoandikiwa	Uandikaji Ulikamilishwa (W.K.)	Muda Unaohusika
Mathayo	Mathayo	Palestina	m. 41	2 K.W.K.–33 W.K.
Marko	Marko	Roma	m. 60-65	29-33 W.K.
Luka	Luka	Kaisaria	m. 56-58	3 K.W.K.–33 W.K.
Yohana	Mtume Yohana	Efeso, au karibu	m. 98	Baada ya utangulizi, 29-33 W.K.
Matendo	Luka	Roma	m. 61	33–m. 61 W.K.
Waroma	Paulo	Korintho	m. 56	
1 Wakorintho	Paulo	Efeso	m. 55	
2 Wakorintho	Paulo	Makedonia	m. 55	
Wagalatia	Paulo	Korintho au Antiokia ya Siria	m. 50-52	
Waefeso	Paulo	Roma	m. 60-61	
Wafilipi	Paulo	Roma	m. 60-61	
Wakolosai	Paulo	Roma	m. 60-61	
1 Wathesalonike	Paulo	Korintho	m. 50	
2 Wathesalonike	Paulo	Korintho	m. 51	
1 Timotheo	Paulo	Makedonia	m. 61-64	
2 Timotheo	Paulo	Roma	m. 65	
Tito	Paulo	Makedonia (?)	m. 61-64	
Filemoni	Paulo	Roma	m. 60-61	
Waebrania	Paulo	Roma	m. 61	
Yakobo	Yakobo (ndugu ya Yesu)	Yerusalemu	k. 62	
1 Petro	Petro	Babiloni	m. 62-64	
2 Petro	Petro	Babiloni (?)	m. 64	
1 Yohana	Mtume Yohana	Efeso, au karibu	m. 98	
2 Yohana	Mtume Yohana	Efeso, au karibu	m. 98	
3 Yohana	Mtume Yohana	Efeso, au karibu	m. 98	
Yuda	Yuda (ndugu ya Yesu)	Palestina (?)	m. 65	
Ufunuo	Mtume Yohana	Patmosi	m. 96	

[Majina ya waandikaji wa vitabu fulani na ya mahali fulani vilipoandikiwa si hakika. Tarehe nyingi zimekadiriwa tu, alama b. inamaanisha “baada ya,” k. inamaanisha “kabla ya” na m. inamaanisha “mnamo” au “karibu.”]

[[ ]] Mabano mawili yanaonyesha kwamba maneno ya ziada yamepachikwa ndani ya maandishi ya kwanza.

FAHIRISI YA BAADHI YA MANENO YA BIBLIA

Angalia ukurasa wa 6 uone ufupisho wa majina ya vitabu vya Biblia

A

ABADONI, Ufu 9:11 mfalme, jina lake ni *Abadoni*
ABBA, Ro 8:15 tunapaaza sauti: *Abba,* Baba!
Ga 4:6 roho hupaaza kilio: *Abba,* Baba!
ABEDNEGO, Da 1:7 Azaria akamwita *Abednego*
Da 2:49; 3:12, 30.
ABELI, Mwa 4:4 Yehova akimtazama *Abeli*
Mt 23:35 damu ya *Abeli* mwadilifu
Ebr 11:4 Kwa imani *Abeli* alitoa dhabihu
Mwa 4:2, 8, 25; Lu 11:51; Ebr 12:24.
ABIHU, Kut 6:23 Nadabu na *Abihu*
Law 10:1; Hes 3:4.
ABIMELEKI, Mwa 20:2 *Abimeleki* mfalme
Amu 9:16; 2Sa 11:21.
ABISHAI, 1Sa 26:6 *Abishai* mwana wa Seruya
2Sa 21:17; 23:18.
ABISO, Ufu 20:3 akamtupa ndani ya *abiso*
Lu 8:31 asiwaagize waingie katika *abiso*
Ro 10:7 nani atakayeshuka katika *abiso*
Ufu 9:1, 11; 11:7; 17:8.
ABIYA, 1Sa 8:2; 1Fa 14:1; Lu 1:5.
ABNERI, 1Sa 14:50; 20:25; 2Sa 3:20.
ABRAHAMU, Mwa 17:9 *Abrahamu:* shika agano
